انواع السجود في الاءسلام وكيفيتها

الجزء الاول

SUJUUD

AINA ZAKE NA UTEKELEZWAJI WAKE KATIKA UISLAM - JUZUU YA KWANZA.

تجميع وانتاج
المستكشف أبومنال دانا

KIMETAYARISHWA NA AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH
Rabiu Al Akhir, 1447 A.H – Oktoba, 2025 C.E

انواع السجود في الاءسلام وكيفيتها

SUJUUD

Aina Zake Na Utekelezwaji Wake.

Katika Uislam.

Juzuu ya Kwanza

تجميع وانتج

المستكشف ابو منال دانا

Kimetayarishwa Na Al Mustakshif Abu Manal Danah.

Rabiu Al Akhir, 1447 A.H – Oktoba, 2025 C.E

YALIYOMO

YALIYOMO *3*
VITABU VILIVYOTANGULIA VYA AL MUSTAKSHIFABU MANAL DANAH: *7*
UTANGULIZI *8*
MAANA YA SUJUD NA AINA ZAKE KATIKA UISLAM *12*
MANUFAA YA SUJUD *13*
AINA ZA SUJUD *17*
1 - AL SUJUUD FII SALAT *20*
2 - SUJUD AL SHUKR *24*
3-SIJDAT AL TILAWAH *26*
AYA ZA SIJDA NDANI YA QUR'AN *30*
HUKMU ZA SIJDAT AT TILAWAH *36*
4-SIJDAT AS SAHW *38*
ARKANU SALAAT - NGUZO ZA SALA *43*
1-AN NIYYAH *55*
KUBADILISHA NIA YA SALA NDANI YA SALA. *62*
NIYYAH YA SALA ZA FARDHI NA SUNNAH NA MASHARTI YAKE. *66*
2-TAHARRUM - TAKBIRAT AL IHRAM *69*
MASHART YA TAHARRUM - TAKBIRAT AL IHRAM *72*
RAF AL YADAIN *75*
3-AL QIYYAM *82*
ASIEWEZA KUSIMAMA WALA KUKAA KATIKA SALA. *93*
MTIZAMO WA MACHO KATIKA SALA *95*
ISTAW – KUGUSANISHA VIDOLE VYA MIGUU NI SUNNA AMA LA? *99*
KUFUNGA MIKONO *105*
KUFUNGA MIKONO AU KUTOFUNGA BAADA YA RUKUU? *114*
TAWAJJUH –DUA IFTITAH AU DUA ISTIFTAAH *117*
AT TA'AWWUDH –AUDHU BILLAHI MINA AL SHAYTANI RAJIIM *123*
TASMIYAH - BIISMI ALLAHI RAHMANI RAHIM *134*
4 - QIRAAT SURAT AL FATIHA *151*
KUSOMAQUR'AN KWA KUTUMIA MSAHAFU NDANI YA SALA. *173*
KUITIKIA AMIIN BAADA YA KISOMO CHA SURAT AL FATIHA *180*
KISOMO CHASURA NYENGINE BAADA YA SURAT AL FATIHA KATIKA SALA *183*
5-RUKUU *189*
ADHKARI ZA RUKUU *193*
UKAMILIFU WA RUKUU *199*
SIRI YA RUKUU *205*

6-ITIDAL AL QAWMA KISIMAMO CHA BAADA YA RUKUU 210
KWANINI HAKUNA TAKBIRAT AL INTIQAL BAADA YA RUKUU 214
MASHARTI YA ITIDAL AL QAWMA 222
7-SUJUD 226
KUTANGULIZA CHINI MIGUU AU MIKONO KWANZA KATIKA SUJUD? 229
UMUHIMU WA KUGUSISHA PAJI LA USO NA PUA ARDHINIKATIKA SUJUD 232
SUJUD –MASHARTI 7 YA KUSUJUDU 242
SUJUD KATIKA MAENEO YA KANISANI, HEKALUNI, MAZIZINI, NJIANI N.K. 246
SUJUD KATIKA SEHEMU YA ARDHI ILIYOPORWA 249
KUSALI NA KUSUJUDU JUU YA KITU KILICHOTANDIKWA 258
MIKONO NA MIGUU KATIKA SUJUD 264
ADHKAR ZA SUJUD 280
QUR'AN KATIKA SUJUD 290
DUA KATIKA SUJUD 292
DUA KWA LUGHA ISIYOKUA YA KIARABU NDANI YA SUJUD 298
8-ITIDAL BAYNA SIJDATAYN 310
9-TMAI'NINAH KUTULIA BAINA YA SIJDA MBILI 319
ADHKAR BAINA SIJDA MBILI 321
SIJDA YA PILI NA UKAMILIFU WA RAKAA. 330
HIKMA YA KURUDIA RUDIA HATUA ZA KILA RAKAA YA SALA 334
MAVAZI YA YANAYOBATILISHA SUJUD. 337
HUKMU YA KUONEKANA KWA MIGUU YA MWANAMKE KATIKA SUJUD 340
SIJDA JUU YA MGONGO WA MTU NDANI YA SALA. 342
SUJUD NA MANUFAA YAKE KWA AFYA YA IBN ADAM. 344
JALASAH AL ISTIRAAHA KIKAO BAADA YA SIJDA YA PILI 347
NAMNA YA KUNYANYUKA BAADA YA JAALASAT AL ISTIRAAHA 360
KUKANDA UNGA BAADA YA JAALASAT AL ISTIRAAHA 362
10-TAHIYYAT - TASHAHUD MAANA YAKE NA ASILI YAKE 366
AINA ZA TASHAHUD/TAHIYYAT 377
HUKMU ZA TASHAHUD/TAHIYYAT KATIKA SALA. 392
KUNYOOSHA KIDOLE KATIKATASHAHUD/TAHIYYAT YA SALA. 402
JEE TAHIYYAT YA MWANZO NI WAJIB AMA SUNNAH? 409
KISIMAMO BAADA YA TAHIYYAT YA PILI 410
11-KIKAO CHA TAHIYYAT YA MWISHO. 412
SALAT IBRAHIMIYYAH NA MANUFAA YAKE 414
DUA KATIKA KIKAO CHA TAHIYYAT YA MWISHO. 424
12-TASLIM – KUTOA SALAM 435

13-TARTIB – KUFUATISHA UTARATIBU.....442
TMA'ININAH.....445
SUNNAN AB'AADH.....451
QUNUT – KATIKA SALATAL FAJIR......457
MUFARRAQAH NA HUKMU YAKE KATIKA SALA.....474
HUKMU YA KUNYANYUA MIKONO KATIKA DUA YA QUNUT.....485
QUNUT – KATIKA SALAT AL WITR YA MWEZI WA RAMADHAN......492
QUNUT NAZILA.....502
SALAT AN NABII KATIKA QUNUT.....512
SUNNAN HAI'AT.....516
NAMNA YA KUITEKELEZA SIJDAT SAHW.....524
HUKMU YA SIJDAT SAHW.....536
HUKMU YA KUA NA SHAKA NDANI YA SALA.....549
YALIYORUHUSIKA NDANI YA SALA - JUU AU NDANI YA KIPANDO.....561
YALIYORUHUSIKA NDANI YA SALA KATIKA WAKATI WA KHOFU......575
YALIYORUHUSIKA NDANI YA SALA – JAM'AA- KUJUMUISHA SALA.....583
YALIYORUHUSIKA KATIKA ADHANA YA KUJUMUISHA SALA......596
YALIYORUHUSIKA KUKATISHA SALA......599
MUBTILATAL SALAT - YANAYOBATILISHA SALA.....616
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- HADATH.....616
MANUFAA YA UDHU KIMWILI NA KINAFSI.....621
TAYAMMAM.....637
TAYAMMAM NA HUKMU ZAKE.....659
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- DAMAN MASFUUHAN.....674
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- HEDHI.....687
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- ISTIHADHAH.....693
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- NIFAS.....697
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MANII......704
GHUSL -KUJITOHARISHA KWA KUKOGA KOGO LA JANABA.....735
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MADHII......750
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MADHII KWA MWANAMKE.....763
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- RUTUBAT AL FARJ.....768
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MADII.....774
ISTIBRA, NATR NA NADH KATIKA KUJITOHARISHA.....779
MANII NA RUTUBAT AL FARJ NI TOHARA; JEE INARUHUSIKA KUMEZWA?.....783
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- HAJA NDOGO NA KUBWA.....790
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MKOJO WA NGAMIA.....795

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MKOJO WA PAKA.....799
UMMUM UL BALWA NA MUBTILAT SALAT.....800
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- KINYESI CHA NDEGE.....804
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MANYOYA YA NDEGE.....807
MUBTILAT SALAT – MAA'DHUR KUTENGUKA KWA UDHU KWA WENYE UDHURU. 814
MUBTILAT SALAT – MAA'DHUR BILA YA MAJI NA MCHANGA WA KUJITOHARISHA.....819
MUBTILAT SALAT- MAADHUR MWENYE MFUKO WA MKOJO 825
MUBTILAT SALAT – MAA'DHUR MWENYE BENDEJ AU PLASTA 828
MUBTILAT SALAT – KUJIGUSA SEHEMU ZA SIRI 835
MUBTILAT SALAT – KUGUSANA NA JINSIA NYENGINE. 847
MUBTILAT SALAT - KUGUSANA NA JINSIA NYENGINE KATIKA IBADA YA HIJA 877
MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- KUPOTEZA UFAHAMU 895
MUBTILAT SALAT – IRTIDDAD - KUTOKA KWENYE UISLAM 910
MUBTILAT SALAT – KUCHAKUA, KULA NA KUNYWA.....933
MUBTILAT SALAT – KUCHAKUA, KULA NYAMA YA NGAMIA 941
MUBTILAT SALAT – NAJIS YA NGURUWE.....951
MUBTILAT SALAT – NAJIS YA NGURUWE NA AL ISTIHALAH.....969
MUBTILAT SALAT – NAJIS YA MBWA.....977
MUBTILAT SALAT – JEE INARUHUSIKA KUFUGA MBWA.....986
MUBTILAT SALAT – JEE INARUHUSIKA KUUZA NA KUNUNUA MBWA.....1006
MARUDIO YA VITABU VILIVYOTUMIKA KATIKA KUANDAA KITABU HIKI.....1016

VITABU VILIVYOTANGULIA VYA AL MUSTAKSHIFABU MANAL DANAH:

1-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAM NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA KWANZA - MWAKA - *1435 AL HIJRA* (2014).

2-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAM NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA PILI - MWAKA - *1437 AL HIJRA* (2016).

3-IJTIHAD NA TAQLID HISTORIA YA UISLAM: MAIMAM NA MADHHAB YAO KATIKA UISLAM - TOLEO LA TATU - MWAKA *1439 AL HIJRA* (2018).

4-TAFSIR SURAT YUSUF – AHSAN AL QASAS - MWAKA *1441 AL HIJRA* (2020).

5-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL AWWAL – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA KWANZA – MWAKA 1442 AL HIJRA (2021).

6-ULU UL AZMI MINNA RUSULUN JUZUU AL THANI – WENYE AZMA THABIT MIONGONI MWA MITUME JUZUU YA PILI – MWAKA 1443 AL HIJRA (2022).

7-TABAQAT WARATHAT AL ANBIYAI - AL JUZUU Al AWWAL - MATABAKA YA WARITHI WA MITUME -JUZUU YA KWANZA - MWAKA 1443 AL HIJRA (2022).

8- TAFSIR YA SURAT AL KAHFMWAKA 1444 AL HIJRA (2023).

9-HAZINAT MUJARRABAT AL QADHIYAT AL HAJJAT(2023)

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

UTANGULIZI

❖❖❖❖

﴿بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ نَحْمَدُهُ ونَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُضْلِلْ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Inna Al hamda Lillaahi nahmaduhu wanasta'eenahu wa nastaghfiruhu, wa na'oodhu billaahi min shuroori anfusinaa wa min sayi'aati a'maalinaa. Man yahdih - Illaahu falaa mudhilla laahu wa man yudhlil falaa haadiya lahu. Wa ashhadu an laa ilaaha ill-Allaahu wahdahu laa shareekallahu, wa ashhadu anna Muhammadan 'Abduhu wa Rasooluhu.

*Tafsir:**Kwa jina la Allah, ambae anastahiki shukrani zote, tunaemuomba msaada na msamaha wake. Tunajilinda kwa ulinzi wa Allah na kila maovu ya Nafsi zetu na mambo mabaya yetu. Kwani kwa hakika mtu yeyote yule alieongozwa na Allah basi hakuna atakaempotoa, na aliepotoshwa na Allah basi hakuna atakaemuongoa. Nnashuhudia kua hakuna anaepaswa kuabudiwa isipokua Allah pekee asiekua na mshirika, na nnashuhudia kua Muhammad (Salallahu A'layhi wa Salam) ni Mja wake na ni Mtume wake.***

يقول الله عز وجل في كتابه العزيز

﴿يأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha haqqa tuqatihi wala tamootunna illa waantum muslimoona *(Surat Al Imran 3:102)*

*Tafsir: **Enyi mlioamini! Muogopeni Allah (kwa kutekeleza maamrisho yake na kuachana na makatazo yake) kama anavyostahiki kuogopewa. [Mtiini, mshukuruni na daima mkumbukeni], na msife isipokua mkiwa katika hali ya kua ni Waislam.***

﴿يَأَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُواْ رَبَّكُمُ الَّذِى خَلَقَكُمْ مِنْ نَّفْسٍ وَحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالاً كَثِيراً وَنِسَآءً وَاتَّقُواْ اللَّهَ الَّذِى تَسَآءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيباً﴾

Ya ayyuha alnnasu ittaqoo rabbakumu alladhi khalaqakum min Nafsin wahidatin wakhalaqa minha zawjaha wabaththa minhuma rijalan kathiran wanisaan waittaqoo Allaha alladhii tasaaloona bihi waAl arhama inna Allaha kana AAalaykum raqeeban *(Surat An Nisaa 4:1)*

*Tafsiri: **Enyi Watu! Mcheni Mola wenu aliekuumbeni kutokana na Nafsi moja (Adam), na kutokana nae (Adam) akamuumba mke wake (Hawwa), na kutokana nao (Adam na Hawa) akawaumba***

Wanaume na Wanawake wengi na muogopeni Allah ambae ana haki juu yenu, na msivunje udugu, kwani kwa Hakika Allah ni mwenye uangalifu mkubwa juu yenu.

﴿يأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ وَقُولُواْ قَوْلاً سَدِيداً ۞ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَلَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزاً عَظِيماً﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha waqooloo qawlan sadeedan, Yuslih lakum aAAmalakum wayaghfir lakum dhunoobakum waman yutiAAi Allaha warasoolahu faqad faza fawzan AAadhiman*(Al Ahzab 33:70-71)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini! mcheni na muogopeni Allah, na (daima) semeni kauli za ukweli ulionyooka, atakuongozeni kufanya mema na kukusameheni dhambi zenu. Na kwa hakika yeyote yule ambae anaemtii Allah na Mtume wake (Salallahu A'layhi wa Salam) basi atakua ni miongoni mwa waliofuzu kwa Darja kubwa.***

Allahuma Ij'Aalna minna al faizin fawzan A'adhimah…Aamin

أَمَا بَعْدُ

قال الله عز وجل

﴿ وَمِنْ آيَاتِهِ ٱللَّيْلُ وَٱلنَّهَارُ وَٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ لاَ تَسْجُدُواْ لِلشَّمْسِ وَلاَ لِلْقَمَرِ وَٱسْجُدُواْ لِلَّهِ ٱلَّذِى خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴾

Wamin ayatihi allaylu waalnnaharu waalshshamsu waalqamaru la tasjudoo lilshshamsi wala lilqamari waosjudoo lillahi aladhee khalaqahunna in kuntum iyyahu taAAbudoona(Surat Fusilat 41:37)

Tafsir ***Na Katika Aya /Daliki Zake(Ni katika Kuumba) Ni Mchana na Usiku Na Jua na Mwezi Hivyo Msisujudie (Viumbe) Kwa ajili ya Jua wala kwa ajili ya Mwezi Bali Sujudieni Kwa Allah Ambae Ndie Alieviumba (Hivyo Viumbe vyake)-Kama Ikiwa Kweli Nyinyi Mnamuabudu yeye (Allah Subhabah wa Ta'ala)***

Na akasema tena kua:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ إِذَا قُمْتُمْ إِلَى ٱلصَّلاةِ فٱغْسِلُواْ وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى ٱلْمَرَافِقِ وَٱمْسَحُواْ بِرُؤُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى ٱلْكَعْبَينِ وَإِن كُنتُمْ جُنُباً فَٱطَّهَّرُواْ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىَ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ ٱلْغَائِطِ أَوْ لاَمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيداً طَيِّباً فَٱمْسَحُواْ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِّنْهُ مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo idha qumtum ila alssalati faighsiloo wujoohakum waaydiyakum ila almarafiqi waimsahoo biruoosikum waarjulakum ila alkaAAbayni wa-in kuntum junuban

faittahharoo wa-in kuntum mardha aw AAala safarin aw jaa ahadun minkum mina algha-iti aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban faimsahoo biwujoohikum waaydeekum minhu ma yureedu Allahu liyajAAala AAalaykum min harajin walakin yureedu liyutahhirakum waliyutimma niAAmatahu AAalaykum laAAallakum tashkuroona*(Surat Al Maidah 5:06)*

Tafsir: ***Enyi wale ambao mlioamini! Mnapotaka kufanya Ibada ya Sala, basi kosheni Nyuso zenu na mikono yenu hadi kwenye visugudi, pitisheni mikono yenu (iliyoroa maji) kwenye vichwa vyenu na kosheni miguu yenu hadi juu kwenye viungio vya visigino. Na kama mkiwa mko katika hali ya Janaba, basi jitoharisheni kwa kukoga. Lakini kama mkiwa mnaumwa au mko safarini au mmoja wenu akiwa amejisaidia au ikiwa mmegusana na Mwanamke na hamkupata Maji, basi fanyeni Tayammam kwa kutumia Mchanga msafi na panguseni nyuso zenu na mikono yenu kutokana nao. Allah hataki kukuwekeni katika hali ya kua na ugumu na anataka kukutoharisheni na kukukamilishieni neema zake juu yenu ili mpate kua ni wenye Shukurani.***

Na amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿فَإِذَا قَضَيْتُمُ ٱلصَّلاَةَ فَٱذْكُرُواْ ٱللَّهَ قِيَاماً وَقُعُوداً وَعَلَىٰ جُنُوبِكُمْ فَإِذَا ٱطْمَأْنَنتُمْ فَأَقِيمُواْ ٱلصَّلاَةَ إِنَّ ٱلصَّلاَةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَاباً مَّوْقُوتاً﴾

Fa-idha qadhaytumu alssalata faodhkuroo Allaha qiyaman waquAAoodan waAAala junoobikum fa-idha itma/nantum faaqeemoo alssalata inna alssalata kanat AAala almu/mineena kitaban mawqootan*(Surat An Nisaa 4:103)*

Tafsir: ***Na mtakapomaliza Kusali basi mkumbukeni Allah mkiwa mmesimama, mkiwa mmekaa na mkiwa mmelala kwa ubavu mmoja, na mnapokua Salama basi Salini, kwani kwa hakika Sala imeamrishwa juu ya Walioamini kwa Nyakati zake maalum.***

Alhamd lillah Rabi Al Alamin, wa Salatu wa Salamu Aala Rasulu Allah Salallahu Alayhi Wa Salam, wa Aala Aliihi Wa As-habihi, wa Tabiin wa Al Awliya wa al ulamaa wa Muslimin Ajmaain.

Namshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kuniwezesha kwa mara nyingine tena kuandaa kitabu chengine kama hiki chenye malengo ya kuukumbusha Ummah wa Kiislam kuhusiana na baadhi ya yale wasiyoyajua, waliyoghafilika nayo na pia waliyoyasahau, kwa baadhi yetu miongoni mwao kuhusiana na Ibada zao.

Hiki ni kitabu ambacho ndani yake ni chenye kuzungumzia kuhusiana na Sujud na aina zake na utakelezwaji wake katika Imani ya Dini ya Kiislam kama linavyojielezea Jina la Kitabu hiki, na kwa kua Sujud ni Ibada katika Imani ya Dini ya Kiislam na kuna Sujud ambazo ni zenye kuenda sambamba na Ibada ya Sala ya kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni moja kati ya Nguzo Tano za Dini ya Kiislam basi nimeamua kuelezea pia baadhi ya mambo ambayo yanaendana sambamba na Ibada mbili hizo kwa ajili ya Kuwaelimisha na kuwafafanulia zaidi wale wasiojua kuhusiana na Ibada hio kwa kukigawa kitabu hiki katika Juzuu mbili tofauti.

Namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atunufaishe kwa kila jema na lenye manufaa liliomo ndani yake kitabu hiki na pia atuepushe na kila lisilokua na manufaa na lenye kasoro ndani yake, kwani ukamilifu ni wake pekee *Allah Subhanah wa Ta'ala* na yeye ndie pekee mwenye kustahiki Shukrani kutokana na Neema na Rehma yake juu yet ya kutujaalia sisi kua ni miongoni mwa wafuasi wa Dini yake ya Kiislam.

SUBHANA ALLAH W ALHAMD LILLAH!

MAANA YA SUJUD NA AINA ZAKE KATIKA UISLAM

❖❖❖❖

Neno *Sajada* kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kusjudu, Kuinama mpaka Chini, Kua katika Hali ya Chini, Kuinamisha Kichwa hadi kikagusa Ardhi, Kuinamisha Kichwa Hadi Paji la Uso na Pua vikawa ni vyenye kugusa Ardhi, Kua Mnyenyekevu,Kuonesha Heshima ya Hali ya Juu kabisa.

Anasema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:**'*Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Nimeamrishwa mimi kusjudu kwa kutumia mifupa saba ya mwili ambayo ni Paji la Uso pamoja na ncha ya Pua.' na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaigusa Pua yake. Kisha akaendelea kusema:'Kwa kutumia Viganja vya mikono yote miwili, Magoti yote Mawili, na Vidole vya miguu yote miwili, na kutojali kuhusiana na Nguo wala Nywele zitakavyokaa.'***(Bukhari na Muslim)*

Naam..neno Sajada Ndio lililotoa neno *Masjidun* ambalo humaanisha Masjidi, Msikitini au Sehemu ya Kufanyia Ibada ya Kumuabudu *Allah Subhabah wa Ta'ala.*

Ambapo amesema Abd Allah Ibn Abi Awfa *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Wakati Muadh Ibn Jabal alipowasili kutoka nchini Sharia basi alimsujudia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Na Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema: 'Hivi Jee ndio unafanya nini ewe Muadh?'**

Ambapo Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ya Rasul Allah! Mimi nimetoka katika Ardhi ya Syria na nimewaona watu wa huko wakiwa Wanawasjudia Mapadri wao na Makasisi wao. Hivyo Na mimi ningependa Kukusjudia wewe Ya Rasul Allah!'

Hivyo R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: La Usifanye hivyo ewe Muadh!

Kwani kama mimi ningekua ni mwenye kuamrisha Watu wawasjudie wengine zaidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ningeamrisha Wanawake wawasjudie Waume zao. Kwani nnaapa mimi kwa yule ambae Ndani ya mikono yake kua Umiliki wa Roho ya Muhammad kua hakuna Mwanammke atakaeweza kutekeleza Majukumu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yake hadi pale atakapoweza kutekeleza Majukumu ya Mume wake juu yake. Kiasi ya kua Mume akimtaka Mke basi hata kama Mke yuko juu ya Kiti cha Ngamia basi Mke wake huyo haruhusiki kumkaatalia Mume wake.'*(Sunan Ibn Majah)***

Na kwa Upande mwengine basi anasema Qays Ibn Saad *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mimi nilienda katika maeneo ya Al Hira na nikawaona watu wa Al Hira wanawasujudia watu wenye Darja kubwa zaidi yao,hivyo nikasema Kwa Hakika *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anastahiki kusujudiwa zaidi kuliko wanavyofanyiwa hawa Hivyo nikarudi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na nikawambia kua:**

***Ya Rasul Allah* hakika mimi nimeenda kwenye maeneo ya Al Hiira na nimewaona watu wanawasjudia watu wao walio bora miongoni mwao Ambapo wewe ni *Rasul Allah* hivyo unastahiki kusjudiwa kuliko wasujudiwavyo wao.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema 'La Msifanye hivyo, kwani kama mimi ningeamrisha watu kuwasujudia wengine basi ningewaamrisha Wake kuwasujudia Waume zao, kwa sababu ya Haki waliyopewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yao'(Imam Al Hakim)***

Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Sujud basi tunaona kua ni kitendo ambacho kina thamani kubwa na manufaa kadhaa.

MANUFAA YA SUJUD

❖❖❖❖

(وَأَمَّا السُّجُودُ فَاجْتَهِدُوا فِي الدُّعَاءِ فَقَمِنٌ أَنْ يُسْتَجَابَ لَكُمْ).

‘Ama sijda, jitahidi sana katika kuomba dua yako, kwani hakika itaitikiwa dua yako.’*(Sahih Muslim)*

Hii ni ni moja kati ya miongoni mwa hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* inayothibitisha umuhimu na Manufaa ya Sujud katika kumsujudua *Allah Subhanah wa Ta’ala.*

Na hiI ni kwa sababu Sujud ni moja kati ya matendo yanayopendwa zaidi na *Allah Subhanah wa Ta’ala* na hivyo kua ni miongoni mwa mambo bora ambayo yatampelekea mwenye kuyafanya kua ni sababu itakayompelekea kuingia Peponi, kama ilivyothibitishwa katika iliyomo katika Sahih Muslim kutoka kwa Maadan Ibn Abi Talha Al Yamari,*Radhi Allahu Anhu*, ambaye amesema:

أخبرني بعملٍ أعمله يدخلني به الجنة، أو قال: قلت: بأحبِّ الأعمال إلى الله، فسكت، ثم سألته، فسكت، ثم سألته الثالثة، فقال: سألت عن ذلك رسولَ الله صلى الله عليه وسلم فقال: «عليك بكثرة السجود لله؛ فإنك لا تسجد لله سجدةً، إلا رَفَعَك الله بها درجة، وحطَّ عنك بها خطيئة»، قال معدان: ثم لقيت أبا الدرداء فسألته فقال لي مثل ما قال ثوبان،

Nilikutana na Thawban *Radhi Allahu Anhu* Mawla *wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nikamwambia: ‘Niambie kitendo nitakachokifanya kitakachoniingiza Peponi, au akasema: “*Ni ipi Amali inayopendwa zaidi na Allah Subhanah wa Ta’ala ?’* Nae akanyamaza, nikamuuliza tena, akanyamaza, kisha nikamuuliza mara ya tatu, Thawban *Radhi Allahu Anhu*akasema: ‘Nilimuuliza *wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na hilo. Na alisema: “Lazima umsujudie *Allah Subhanah wa Ta’ala* mara kwa mara; Humsujudii Mja*Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa sijda, isipokuwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* hukunyanyua daraja moja kwa ajili yake, na kukuondolea dhambi kwa ajili yako, name nikamuuliza Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* ambapo nae akaniambia mimi kama alivyosema Thawban. *(Sahih Muslim).*

Na miongoni mwa manufaa ya Sujud ni kama alivyosema Rabi'ah Ibn Ka'b Al Aslami *Radhi Allahu Anhu* kua, alisema:

كنت أبيت مع رسول الله –صلى الله عليه وسلم– فأتيته بوضوئه وحاجته فقال لي: «سل» فقلت: أسألك مرافقتك في الجنة. قال –صلى الله عليه وسلم–: «أو غير ذلك؟» قلت: هو ذاك، قال: «فأعني على نفسك بكثرة السجود

Nilikuwa nikilala kwa*Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*nikamsaidia kumpelekea Maji kwa ajili ya udhuu wake na haja zake, akaniambia: “Omba.” Nami nikasema: ‘Ninaomba Niwe pamoja nawe Peponi’ . *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*- akasema: "Au kitu kingine?" Nikasema: ‘Ni Hivyo tu’ nae akasema: “Basi jisaidie kwa kufanya Sijda nyingi.’

Na miongoni mwa manufaa ya Sujud ni kama ilivyothibitishwa na Hadith isemayo:

«ما من مسلم يسجد لله سجدة إلا رفعه الله بها درجة وحط عنه سيئة»، وعن عبادة بن الصامت رضي الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: «ما مِن عبد يسجد لله سجدةً إلا كَتَب الله له بها حسنة، وحطَّ عنه بها سيئة، ورفع له بها درجة؛ فاستكثِروا من السجود» (أخرجه ابن ماجه)

"Hapana Muislamu anayemsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* isipokua*Allah Subhanah wa Ta'ala* humpandisha daraja kwa hayo. na humwondolea ubaya." Na kwa uthibitisho wa Ubaidah Ibn Al Samit *Radhi Allahu Anhu,* ambae amesema: 'Amesema *wa Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* ampe amani: "Hakuna mja anayemsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa sijda isipokua*Allah Subhanah wa Ta'ala* anamuandikia jambo jema, na akamuondolea jambo baya, na akampandisha daraja kwa jema hilo. Hivyo sujuduni sana" *(Sunan Ibn Majah).*

Na pia miongoni mwa manufaa ya Sujud ni kua, anaposujudu Ibn Adam, basi Shaytani hujitenga na kulia, kama alivyosema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua:

: إذا قرأ بن آدم السجدة فسجد اعتزل الشيطان يبكي ويقول يا ويله أمر هذا بالسجود فسجد فله الجنة وأمرت أنا بالسجود فعصيت فلي النار

'Kama Ikiwa Ibn Adam akisoma sijda na kusujudu, basi hujitenga Shaytani na kulia. Huku akiwa ni mwenye kusema: 'Ole wake mtu huyu aliamrishwa kusujudu, na akasujudu, kwani yeye makazi yake ni Pepo, wakati mimi niliamrishwa nisujudu, lakini niliasi, na hivyo nitaingia Motoni.'

Miongoni mwa manufaa ya Sujud ni kua Mja aliye karibu zaidi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaposujudu, kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* kua:

إن أقرب ما يكون العبد من الله تعالى أن يكون ساجدًا»، وقال أبو هريرة رضي الله عنه: أقرب ما يكون العبد إلى الله عز وجل إذا سجد فأكثروا الدعاء عند ذلك.

'Mja aliye karibu zaidi na *Allah Subhanah wa Ta'ala ni sujudu,"* na akasema Abu Hurairah *Radhi Allahu Anhu:* 'Jambo linalomkaribisha zaidi mja mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni kusujudu.'

Na amesema *Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu* kua:

قال النبيُّ صلى الله عليه وسلم: «أقربُ ما يكون العبد من ربِّه وهو ساجد؛ فأكثِروا فيه الدعاء

Amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua "Ukaribu anaoweza kua nao mja Mja kwa Mola wake ni pale anapokua ndani ya Sijda; Basi zidisheni maombi ndani yake."*(Sahih Muslim).*

Na miongoni mwa manufaa ya Sujud ni kua ni Alama ya Waumini katika Siku ya Malipo kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuwaambia Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kama inavyosema Hadith ifuatayo:

وأخبرنا عمر بن محمد بن معمر المؤدب ، أن الحافظ أبا البركات عبد الوهاب بن المبارك الأنماطي ، وأبا غالب محمد بن محمد بن أسد العكبري الخرقي قالا : أبنا أبو الحسين عاصم بن الحسن بن عاصم العاصمي ، ثنا أبو عمر عبد الواحد بن محمد بن عبد الله بن محمد بن مهدي ، ثنا أبو محمد عبد الله بن أحمد بن إسحاق المصري قراءة عليه ، ثنا إبراهيم بن أبي داود البرلسي ، ثنا أبو اليمان ، ثنا صفوان بن عمرو ، عن يزيد بن خمير الرحبي ، عن عبد الله بن بسر المازني ، عن رسول الله صلى الله عليه وسلم أنه قال : ما من أمتي من أحد إلا وأنا أعرفه يوم القيامة ، قالوا : وكيف تعرفهم يا رسول الله في كثرة الخلائق ؟ قال : أرأيت لو دخلت صيرة فيها خيل دهم بهم ، وفيها فرس أغر محجل ، أما كنت تعرفه منها ؟ قال : بلى ، قال : أمتي يومئذ غر محجلون من الوضوء

Umar Ibn Muhammad Ibn Muammar Al Mu'addab alitufahamisha kwamba Al Hafiz Abu Al Barakat Abdul-Wahhab Ibn Al Mubarak Al Anmati na Abu Ghalib Muhammad Ibn Muhammad Ibn Asad Al Akbari Al Kharqi alisema: Abu Al Hussein. Asim Ibn Al Hasan Ibn Asim Al Asimi alituambia, Abu Umar Abdul-Wahid Ibn Muhammad Ibn Abdullah Ibn Muhammad Ibn Mahdi alituambia, Abu Muhammad Abdullah Ibn Ahmad Ibn Ishaq Al Masry alitusomea, Ibrahim Ibn Abi Dawud Al Barlisi. alituambia, Abu Al Yaman alituambia, Safwan Ibn Amr alituambia, kwa idhini ya Yazid Ibn Khameir Al Rahbi, kutoka kwa Abdullah Ibn Busr Al Mazini, kwa idhini ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*alisema:

‘**Hapana Hata mmoja katika Umma wangu isipokua nitamjua Siku ya Kiyama. Masahaba *Radhi Allahu Anhum*wakasema: Utawatawajuaje, Ya *Rasul Allah (Salallahu Alayhi wa Salam)*, miongoni mwa wingi wa watu? *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*Akasema: Niambie, lau kamaukiingia mahali ambapo kuna Farasi weusi, na ndani yake kuna Farasi mweusi mwenye miguu myeupe na doa jeupe kwenye paji la uso wake, je, hamtoweza kumjua? Masahaba *Radhi Allahu Anhum*wakasema: Ndiyo tutamjua. *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akasema: Siku hiyo Ummah wangu utakuwa na miguu meupe na paji la uso paji lao jeupe kutokan na udhu.’***(Imam At Tabrani)***

Na kauli ya Imaam Ahmad:‘**Je, hukuijua? Akasema: Ndiyo. Akasema: Umma wangu siku hiyo utang'ara kwa kusujudu, miguu nyeupe na miguu nyeupe kutokana na Udhu.’**

Na katika riwaya ya Al Barlisi: ‘**Lau ungeletwa mfuko ambao ndani yake mna Farasi weusi wenye miguu myeupe, na ndani yake mna Farasi mweupe mwenye miguu myeupe, je, Hmtoweza Kumjua? Masahaba *Radhi Allahu Anhum*wakasema: Ndiyo. *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akasema:: Basi akasema: Umma wangu siku hiyo utang'ara kwa athari za sijda, miguu nyeupe na miguu nyeupe kutokana na Udhu.’**

Al Tirmidhi amepokea mwisho wake kutoka kwa Abu Al Walid Ahmad Ibn Abd Al Rahman Al Dimashqi, kutoka kwa Al Walid Ibn Muslim, na amesema: ‘**Hadithi nzuri, sahihi, ya ajabu kutoka kwenye chanzo hiki. Nami Nikasema: Hadithi hii inakidhi masharti ya Muslim, na Allah Subhanah wa Ta’ala ndiye anajua zaidi, Na pi akuna hadithi isemayo:**

مالك ، عن العلاء بن عبد الرحمن ، عن أبيه ، عن أبي هريرة أن رسول الله صلى الله عليه وسلم خرج إلى المقبرة ، فقال : السلام عليكم دار قوم مؤمنين ، وإنا إن شاء الله بكم لاحقون ، وددت أني قد رأيت إخواننا . قالوا : يا رسول الله ، ألسنا بإخوانك ؟ قال : بل أنتم أصحابي ، وإخواننا الذين لم يأتوا بعد ، وأنا فرطهم على الحوض . قالوا : يا رسول الله ، كيف تعرف من يأتي بعدك من أمتك ؟ قال : أرأيت لو كانت لرجل خيل غر محجلة في خيل دهم بهم ، ألا يعرف خيله ؟ قالوا : بلى يا رسول الله ، قال : فإنهم يأتون يوم القيامة غرا محجلين من الوضوء وأنا فرطهم على الحوض فلا يذادن حوضي كما يذاد البعير الضال ، أناديهم : ألا هلم ألا هلم ألا هلم . فيقال :

Malik, kutoka kwa Al Alaa bin Abdul Rahman, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Abu Hurairah, kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akatoka kwenda makaburini na akasema: Amani iwe juu yako, nyumba ya watu walioamini, na sisi, Allah Subhanah wa Ta'ala akipenda, ningetamani kuwaona ndugu zetu. Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, sisi si ndugu zako?'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akasema: 'La nyinyi ni Masahaba wangu na kuna ndugu zetu ambao bado hawajafika, nami nitawaongoza kwenye bonde.

Masahaba *Radhi Allahu Anhum*wakasema: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* unajuaje atakayekuja baada yako katika Umma wako? *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akasema: 'Mnaonaje kama mtu akiwa na Farasi wenye miguu myeupe miongoni mwa Farasi wake Weusi je, hatajua Farasi wake? Masahaba *Radhi Allahu Anhum*wakasema: Ndio,'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akasema: 'Watakuja Siku ya Kiyama wakiwa wamejaa udhu, na nitakua wa msimamizo wao katika Hodhi, na hakuna mtu yeyote atakaeondolewa katika katika Hodhi langu kama waondolewavyo Ngamia waliopotea bali mimi nitawaita Njooni, njooni, njooni.'

Na miongoni mwa manufaa ya Sujud ni kama Mwenye kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Moto wa Jahannam hautateketeza Paji lake la uso kutokana na athari za sijda yake, kwani amesema Abu Huraira *Radhi Allah Anhu* kua:

: قال النبيُّ صلى الله عليه وسلم: «تأكل النار من ابن آدم إلا أَثَر السجود؛ حرَّم الله على النار أن تأكل أَثَر السجود

Amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*: 'Utamteketeza Moto Ibn Adamu isipokuwa athari za Sijda; *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameuharamisha Moto kuteketeza athari za Sijda.'*(Bukhari na Muslim)***

Na amesema tena *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn *Abbas Radhi Allahu Anhu kua:*

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: «إني نُهيتُ أن أقرأ القرآن راكعًا أو ساجدًا، فأمَّا الركوع، فعظِّموا فيه الرب، وأمَّا السجود، فاجتهِدوا في الدعاء؛ فقَمِنٌ أن يستجاب لكم

Amesema: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Nimekatazwa kusoma Qur'ani nikiwa katika Rukuu au Sujud hivyo mtukuzeni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake, na kuhusu kusujudu jitahidini kuomba; Kwani kwa hakika Mtajibiwa.' *(Sahih Muslim).*

Na miongoni mwa manufaa ya Sujud hua ni moja kati ya sababu zenye kumpelekea Ibn Adam kupataRehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* , kwani mesema *Allah Subhanah wa Ta'ala :*

﴿وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اسْجُدُوا لِلرَّحْمَنِ قَالُوا وَمَا الرَّحْمَنُ أَنَسْجُدُ لِمَا تَأْمُرُنَا وَزَادَهُمْ نُفُورًا﴾

Wa-idha qeela lahumu osjudoo lilrrahmani qaloo wama alrrahmanu anasjudu lima ta/muruna wazadahum nufooran*(Surat Al Furqan 25:60)*

Tafsir: ***Na wanapoambiwa: Msujudieni Mwingi wa Rehema, basi basi husema tumsujudie Mwingi wa Rehema? Na ndio nani huyo Mwingi wa Rehma? Jee unataka tumsujudie yule ambae wewe Muhammad (Salallahu Alayhi wa Salam) Unatuamrisha kumsujudia?***

Hivyo Kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni Kumsujudia Mwingi wa Rehma na hivyo hua ni kuingizwa ndani ya Rehma zake. Na ndio maana aya ikawa haikusema Msujudieni Mola wenu, au Mungu wenu au *Allah Subhanah wa Ta'ala* bali imesema Msujudieni mwingi wa Rehma..

Hayo ndio baadhi ya manufaa ya Sujud na kabla ya kuendelea basi inabidi tufahamishane kua tunapozungumzia kuhusiana na Sujud kimaana basi hua kuna aina zifuatazo za Sujud.

AINA ZA SUJUD

❖❖❖❖

Ama kuhusiana na Sujud ya Aina ya Kwanza ambayo ndio iliyozungumziwa katika Hadith tulizoziangalia hapo kabla ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua kama Yeye angekua ni Mwenye kuamrisha Viumbe kuwasujudia Viumbe wenzao basi angewaamrisha Wake kuwasujudia Waume zao kutokana na Haki za Waume juu ya Wake zao walizopewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yao.

Ambapo ambapo hii hua ni Sujud ya Kiumbe Kuenda Mpaka chini na kisha kugusisha Vidole vya Miguu yake, Magoti yake, mikono yake na Paji lake la Uso na Pua yake kwenye Ardhi huku akiwa mbele ya Yule anaemsujudia na chini yake anaesujudiwa kuonesha Unyenyekevu wa anaesujudia kwa anaesujudiwa.

Na kuhusiana na Aina hii ya Sujud basi kulingana na Vithibitisho vya Hadith tulizoziangalia hapo kabla, tunaona kua hii hua ni aina ya Sujud ambayo Kiumbe hatakiwi kuifanya au kuitekeleza kwa Kiumbe mwenzake yeyote hata kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mwenyewe.Kwani aina hii ya Sujud hua ni kwa ajili ya Muumba tu, ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwa Maana hio basi Yeyote yule atakaefanya Sujud ya aina hii kwa ajili ya Kiumbe mwenzake au kwa ajili ya kitu chengine chochote kile isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Mtu huyo hua tayari ameshafanya Dhambi kubwa kuliko dhambi zote ambayo ni Dhambi ya Shirk yaani ya kumshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hicho alichokisujudia Mtu huyo.

Hivyo kama aliefanya aina hio ya Sujud kwa Mwengine yeyote asiekua *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama Ni Muislam basi hua ni Wajibu wake kufanya Toba ya kweli kwa Mola wake ili amsamehe kosa lake hilo kwani vyenginevyo basi atakua ni miongoni mwa walioangamia hapa Duniani na Akhera pia.

Na juu ya hili kuna Makubaliano ya Ijmaa ya Masahaba na Wanazuoni.Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿ وَمِنْ آيَاتِهِ ٱللَّيْلُ وَٱلنَّهَارُ وَٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ لاَ تَسْجُدُواْ لِلشَّمْسِ وَلاَ لِلْقَمَرِ وَٱسْجُدُواْ لِلَّهِ ٱلَّذِى خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ﴾

Wamin ayatihi allaylu waalnnaharu waalshshamsu waalqamaru la tasjudoo lilshshamsi wala lilqamari waosjudoo lillahi aladhee khalaqahunna in kuntum iyyahu taAAbudoona*(Surat Fusilat 41:37)*

*Tafsir **Na Katika Aya /Daliki Zake(Ni katika Kuumba) Ni Mchana na Usiku Na Jua na Mwezi Hivyo Msisujudie (Viumbe) Kwa ajili ya Jua wala kwa ajili ya Mwezi Bali Sujudieni Kwa Allah Ambae Ndie Alieviumba (Hivyo Viumbe vyake)-Kama Ikiwa Kweli Nyinyi Mnamuabudu yeye (Allah Subhabah wa Ta'ala).***

Kisha kuna aina ya pili ya Sujud ambayo ni ya Kusalimia na Kuonesha Heshima kwa anaefanyiwa Sujud hio.

Na tunapozungumzia aina hii ya Sujud basi inabidi turudi tena kwenye maana ya neno Sujud ambapo tulisema kua moja kati ya maana ya neno Sujud hua ni Kuonesha heshima ya hali ya juu kabisa.Na hivyo aina hii ya Sujud hua inamaanisha Kuinamisha Mwili na kichwa bila ya kushika magoti.Tafakkar!

Kwani anasema Imam Muhammad Ibn Muhammad Murtada Al Zabidi Al Hanafi katika Kamusi yake maarufu ya *Taj Al Arus min Jawahir Al Qamus* kua: '**Neno *Sajada* hua linatumika kuonesha kitendo cha Mtu Mnyenyekevu pale anapokua ameinama kuelekea Chini.'**

Na bila ya shaka wenye Lugha yao hua hawatumii neno Sajada kaa kuelezea hali ya Ibn Adam tu.Bali pia hutumia kuelezea hali ya kupinda na kuinama kwa vitu mbali mbali kwa mfano husema:

Kila Kitu kinacho jinyenyekesha hua kinaambiwa kua ni chenye kufanya Sijida.

Hivyo hata Matawi ya Miti yanapokua yameinama sana hua yanasemwa kua Yamesujudu.

Na hata Tanga la Jahazi linapojaa Upepo na kulisukuma mbele Jahazi kwa kasi basi huambiwa kua Jahazi Limeusujudia Upepo kutokana na kua Jahazi hilo limezidiwa nguvu na Upepo,Kwa hivyo Jahazi linaonesha Unyenyekevu na kujisalimisha kwa upepo.

Na pia Hata Ngamia anapotaka kupandwa na Mtu anaemuendesha basi Ngamia humbidi kuinama ili amuendeshae aweze kupanda na kukaa juu yake, na hivyo kitendo hicho cha Ngamia hua kinaitwa Sajada, n.k.

Kwa maana hio basi Kitendo hiki cha Kitu au Mtu Kuonesha Unyenyekevu mbele ya Mtu au Kitu hua kinafahamika na kujilikana pia kama Sajada. Na kwa aina hii ya pili ya Sujud ambayo ni ya kuonesha heshima hua ni Sujud inayokubalika na kuruhusika kwani aina hii ya Sujud ndio kama ile iliyozungumziwa katika Surat Yusuf pale ziliposema aya:

﴿وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى ٱلْعَرْشِ وَخَرُّواْ لَهُ سُجَّدًا﴾

WarafaAAa abawayhi AAala alAAarshi wakharroo lahu sujjadan*(Surat Yusuf 12:100)*

*Tafsir: **Na Kisha (Yusuf) akawanyanyua Wazee wakeKwenye ArshiNao Wakakimbilia Kusujudia mbele yake.***

Hii ni Aya inayoelezea Tukio alilolofanya Nabii Yaqub na wake zake mbele ya Nabii Yusuf.Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Al Mushaqiqiin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na aya hii kua;

Hapa kuna hali mbili ambazo tunaweza kuziangalia kufafanua maneno haya: katikaAmbapo kwanza ni kua Nabii Yaqub na Wake zake na Watoto wake hawakumsujudia Nabii Yusuf, bali walimsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na hii ni kwa sababu haiingii akilini kua Nabii Yusuf angemruhusu Baba yake Kumsujudia yeye Kwani Baba yake Nabii Yusuf yaani Nabii Yaqub alikua ni Mtume, na ni Mtu Mzima, Mkubwa Kiumri, Kihikma, Kidini, na ni Baba yake Yusuf.

Na maana ya pili ni kua Kaka zake Yusuf ndio waliomsujudia Yusuf wakati wazee wao wakiwa juu ya Arshi.

Na kama tulivyosema kua aina hii ya kuinama hua inajulikana kama hali ya Sujud ambayo hua inakubalika kufanyiwa kwa Viumbe ambapo hali hii pia imeainishwa tena na *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika *Surat Al Baqara* pale aliposema:

﴿وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَٰٓئِكَةِ ٱسْجُدُواْ لِأَدَمَ فَسَجَدُوٓاْ إِلَّآ إِبْلِيسَ أَبَىٰ وَٱسْتَكْبَرَ وَكَانَ مِنَ ٱلْكَٰفِرِينَ﴾

Wa-idh qulna lilmala-ikati osjudoo li-adama fasajadoo illa ibleesa aba waistakbara wakana mina alkafireen*a(Surat Al Baqara 2:34)*

*Tafsir:**Na Wakati tuliposema kuwaambia MalaikaMsujudieni AdamHivyo nao Wakasjudu Isipokua Ibilisi Akakataa na kua na KibriNa Akawa Miongoni mwa Wenye Kukufuru.***

Ambapo aya hii inatuonesha amrisho la *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutaka asujudiwe Kiumbe Adam na Viumbe Malaika baada ya kuumbwa kwake. Na hivyo A*llah Subhanah wa Ta'ala* kuwabainishia Viumbe Malaika na Ibilisi kua Darja yao iko chini kulingana na Darja ya Kiumbe Adam, na pia kumuonesha Kiumbe Adam kua Darja yake ipo juu zaidi ya Viumbe wawili hao, na hapo hapo kumuonesha ni nani aasifa ya kua rafiki yake na ni nani ana sifa ya kua adui yake.

Na hivyo kamwe Sijida hii haimaniishi kua Viumbe Malaika Waliamrishwa kumuabudia Kiumbe Nabii Adam. Kwani anasema Jarrah Allah, Sultan Al Balagha Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kuhusiana na aya hii kua:

Kusjudu Mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni Ibada na kusjudu kwa Malaika mbele ya Adam hua ni kuonesha heshima mbele ya Adam.

Na amesema Al Aalim, Shaykh Ul Islami Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Aad Ibn Hamza Al Ramli Al Ansari Al Shafii kua: '**Kuinama kwa Kumsujudia Shaykh hua hakumaanishi Kumtukuza Shaykh husika kama vile Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala,* yaani kuonesha kua anabudiwa kwani ikiwa Sijida hio inatokana na nia hio ya Kuabudu basi kufanya hivyo hua ni Kufanya Kufuru'***(Nihayat Al Muhtaj li Sharh Al Minhaj)***

Na akasema Imam Zayn Ad Din Ibn Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Bakr Ibn Nujaym Al Hanafi kua: '**Kuwasjudia Viongozi Wenye Ukatili na Uhdalim hua ni Kufuru kama kutatokana na nia ya Kumuabudu, lakini kama kutatokana na nia ya Kumuamkia basi hamna tatizo, na hii ni kulingana na mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni.'***(Bahr Raiq)*

Nadhani hadi hapa itakua tumefahamina kuhusiana na aina za Sijda na nia zake katika Uislam, na kabla kuendelea zaidi basi na tuangalie kisa cha '**Salman Al Farsi ambae siku moja katika kupita kwake**

kwenye Mitaa ya Madina akakutana *na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo moja kwa moja akaenda chini ya miguu na akamsujudia.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam akamwambia Salman Al *Farisi Radhi Allahu Anhu* kua: Usinisujudie Mimi Ewe Salman, bali Msujudie yule ambae ni Mwenye sifa ya Kuishi Milele na Kutokufa.' *(Musnad Imam Ahmad)*

Na kama tulivyosema kua lengo kuu la kuzungumzia kuhusiana na Sujud ni kwa sababu ya kufahamishana kuhusiana na Sujud za Kiibada ambazo ni kwa ajili ya *Allah Subhabah wa Ta'ala.*

Ambapo tunapoangalia kuhusiana na Sujud hizi basi tunaona kua ziko za aina 4 zifuatazo:

1-Sijdat Salat yaani Sijda ya Ndani ya Sala.

2-Sijdat Shukr yaani Sijda ya Shukurani.

3-Sijdat Tilawah yaani Sijda ya Kisomo cha baadhi ya Aya za Qur'an.

4-Sijdat As Sahw yaani Sijda ya Kufidia Kasoro ya Kusahau Ndani ya Sala.

1 - AL SUJUUD FII SALAT

❖❖❖❖

Sujud ya Kawaida ya Ndani ya Sala tano za Fardhi za Kila siku na Sala nyengine za Sunna Ambapo ndani yake Sala hizi basi hua hatuihesabu Sala ya Jeneza yaani Sala ya Maiti.

Kwani Sala ya Maiti ndio Sala pekee ambayo haina Sujud ndani yake.

Na hii ni kwa Sababu ingawa Sala ya Maiti hua inaitwa Sala lakini ukweli hasa ni kua Sala ya Maiti hua ni Dua ya Kumuombea Maiti na Kujiombea Waislam kwa Waislam wanaomuombea, na waliohai na waliotangulia kwa Ujumla, kama tukakavyoona katika sehemu ya pili ya Kitabu hiki.

Lakini pia hapo hapo tusisahau kua hata hio Sala ya Kawaida hua inajumuisha Ibada ya Vitendo vyenye hatua mbali mbali za Mwili kwa mpangilio Maalum aliofundishwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Malaika Jibril kulingana na maamrisho ya *Allah Subhahan wa Ta'ala* ambayo ndani yake vitendo vya Ibada hio hua pia hua mnajumuishwa Dhikr Allah, Visomo Vya Aya za Qur'an, na Maombi ya Dua ambavyo utekelezwaji wake ndani ya Ibada hii hua ni wenye kuhitaji Ikhlasi inayopelekea kwenye kuonesha Unyenyekevu na Utiifu wa Kiumbe mbele ya Muumba wake.

Na bila ya shaka kwa kila Ibn Adam hua anatofautiana na Ibn Adam mwenzake kwa darja ya Ubora kulingana na Ucha Mungu wake na utiifu wake katika kumuadudu Mola wake kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوباً وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓاْ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ﴾

Ya ayyuha alnnasu inna khalaqnakum min dhakarin waontha wajaAAalnakum shuAAooban waqaba-ila litaAAarafoo inna akramakum AAinda Allahi atqakum inna Allaha AAaleemun khabeerun*(Surat Al Hujurat 49:13)*

Tafsir: ***Enyi Watu! Hakika tumekuumbeni kutokana na Mwanamme mmoja na Mwanamke mmoja na kisha tukakujaalieni (kua katika) Mataifa (tofauti) na Makabila (Tofauti) ili mpate kujuana. Kwa hakikamwenye ubora zaidi miongoni mwenu mbele ya Allah Subhanah wa Ta'ala ni yule Mwenye Ucha Mungu zaidi miongoni mwenu, kwa Hakika Allah ni mwenye kujua juu ya kila kitu na ni mwenye kua na habari juu ya kila kitu.***

Hivyo mwenye ubora zaidi mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni yule mwenye kujitahid katika utekelezaji wa Majukumu yake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kumuabudu, kuachana na makatazo yake na kufanya amali njema zitakazompeleka kupata darja kubwa na ya juu zaid katika Akhera kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

: إن في الجنة مائة درجة، أعدها الله للمجاهدين في سبيل الله، ما بين الدرجتين كما بين السماء والأرض، فإذا سألتم الله فاسألوه الفردوس، فإنه أوسط الجنة، وأعلى الجنة.

'Hakika ya Peponi kuna Darja mia, ambazo zimeandaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa ajili ya Wanaojitolea kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* , na ukubwa wa masafa ya kila moja baina yake ni sawa na masafa ya baina ya Mbingu na Ardhi, hivyo mkimuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi muombeni Firdaws kwani hio ni Pepo ya Katikati baina ya Pepo nandio Pepo ya Juu kabisa'*(*Imam Al Bukhari)*

Na aliulizwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kua:

أي الناس أفضل؟ فقال: مؤمن يجاهد في سبيل الله بنفسه وماله، قالوا: ثم من؟ قال: مؤمن في شعب من الشعاب يتقي الله، ويدع الناس من شره

'Hivi Jee Ni Mtu gani ndio bora zaidi miongoni mwa Watu?'*Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* akasema: Ni Muumini mwenyekupigania kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa maisha yake na mali yake.' Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakauliza tena: 'Na kisha anafutaia nani?'*Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*Akasema: Ni Muumini anaekimbilia Mabondeni kwa ajili yakumcha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kujilinda dhidi ya maovu ya watu.'

Na amesema Abu Kabishah Al Anmari *Radhi Allahu Anhu* kua

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: مثل هذه الأمة كمثل أربعة نفر: رجل آتاه الله مالا وعلما فهو يعمل بعلمه في ماله، ينفقه في حقه، ورجل آتاه الله علما ولم يؤته مالا، فهو يقول: لو كان لي مثل هذا عملت فيه مثل الذي يعمل، قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: فهما في الأجر سواء، ورجل آتاه الله مالا ولم يؤته علما، فهو يخبط في ماله ينفقه في غير حقه، ورجل لم يؤته الله علما ولا مالا، فهو يقول: لو كان لي مثل هذا عملت فيه مثل الذي يعمل، قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: فهما في الوزر سواء.

'Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam **alisema kua: 'Mfano wa Ummah wangu ni sawa na mfano wa watu wanne: Mtu wa kwanza ni yule aliepewa mali na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na**

akapewa na Ilm, hivyo nae akaifanyia kazi Ilm yake na Mali yake kwa kuivitumia vitu hivyo katika njia sahih'

Na kisha Mtu wa pili ambae hakupewa Mali lakini amepewa Ilm, na akamuona mwenzake huyo na hivyo akasema: 'Hakika mimi kama ningejaaliwa Mali kama huyu basi na mimi nigefanya kama afanyavyo yeye.' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Watu hawa wawili hua wanapata malipo sawia katika Mema.'

Na mfano wa Mtu wa Tatu ni wa mtu aliepewa Mali lakini hakupewa Ilm, na hivyo akaitumia Mali hio katika njia zisizokua sahih, na kisha mtu wa nne ambae yeye hakujaaliwa Mali wala Ilm na kisha akamuona mwenzake huyo na kusema: 'Hakika mimi kama ningejaaliwa Mali kama alivyojaaliwa huyu basi na mimi ningefanya kama afanyavyo yeye'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Watu hawa wawili hua wanapata malipo sawia katika Dhambi.''*(Sunan Ibn Majah, Sunan At Tirmidhi, Musnad Imam Ahmad)***

Ambapo hata hivyo chochote kile atakachokifanya Ibn Adam katika utekelezaji wa Majukumu yake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kumuabudu na kutekeleza Amali njema hua ni kutokana na Fadhila na Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* , kwani ni kutokana na fadhila na Rehma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndio kunakompelekea Mja kua ni mwenye kuupata uongofu na kuufuata muongozo wake katika maisha yake kama zinavyosema aya:

﴿وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَاتَّبَعْتُمُ الشَّيْطَانَ إِلَّا قَلِيلًا ﴾

Walawl<u>a</u> fa<u>dh</u>lu All<u>a</u>hi AAalaykum wara<u>h</u>matuhu laittabaAAtumu alshshayt<u>a</u>na ill<u>a</u> qaleel<u>a</u>n.*(Surat An Nisaa 4:83)*

*Tafsir: **Na kama si fadhila za Allah Subhanah wa Ta'ala juu yenu na Rehma zake basi nyote mngekua ni wenye kumfuata Shaytani isipokua wachache tu miongoni mwenu.***

Na akasemA tena kua:

﴿وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَى مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ أَبَدًا وَلَكِنَّ اللَّهَ يُزَكِّي مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ﴾

Walawl<u>a</u> fa<u>dh</u>lu All<u>a</u>hi AAalaykum wara<u>h</u>matuhu m<u>a</u> zak<u>a</u> minkum min a<u>h</u>adin abadan wal<u>a</u>kinna All<u>a</u>ha yuzakkee man yash<u>a</u>o waAll<u>a</u>hu sameeAAun AAaleemun*.(Surat Nur 24:21)***

*Tafsir: **Na kama si fadhila za Allah Subhanah wa Ta'ala juu yenu na Rehma zake hakuna hata mmoja ambae angelikua msafi miongoni mwenu. Lakini Allah Subhanah wa Ta'ala humsafisha amtakae na kwa hakika Allah Subhanah wa Ta'ala ni mwingi wa Kusikia kila kitu na ni mwenye kujua juu ya kila kitu.***

Ambapo anasema Imam Abu Farash Abd Rahman Ibn Ali Ibn Muhammad Ibn Al Jawzi kua: 'Hata kama mtu atakua na Ilm iliyokamilika, basi hatoweza kuongoka kutokana na matendo yake, na kamwe hatoweza kuziona amali zake zote kua ni zenye kutokana nae bali atakua ni mwenye kuziona Fadhila na Rehma za yule ambae ni mwenye kujaalia mafanikio kutokana na matendo mema yake hayo, ambako hua ni kwenye kumzuia mtu mwenye hikma kuyaona

mafanikio ya matendo yake kua niyenye kutokana na yeye mwenyewe ndani ya Nafsi yake au kuvutiwa na matendo yake hayo na hii ni kutokana na kua ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie anaefanikisha matendo hayo.'

Kwani ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie anaeipendezesha Imani ndani ya Waja wake awapendao kwa alivyosema kwenye kitabu chake kitukufu kua:

﴿ يَمُنُّونَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُواْ قُل لاَّ تَمُنُّواْ عَلَيَّ إِسْلاَمَكُمْ بَلِ ٱللَّهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ هَداكُمْ لِلإِيمَانِ إِنُ كُنْتُمْ صَادِقِينَ﴾

Yamunnoona AAalayka an aslamoo qul la tamunnoo AAalayya islamakum bali Allahu yamunnu AAalaykum an hadakum lil-eemani in kuntum sadiqeena.*(Al Hujurat: 49:17)*

*Tafsir**; Na wanakuchukulia kua kama ni fadhila juu yako kua wamesilimu, waambie kua: 'Msihesabu Uislamu wenu kua ni fadhila kwangu mie, bali ni Allah Subhanah wa Ta'ala ndie alie kufadhilini nyie, na hiyvo kukuongozeni katika Imani, kama kweli nyinyi ni wenye kusadiki'***

Kwani kama zitahesabiwa Neema na Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya kiumbe basi Ibn Adam hatofikisha hata asilimia 10 kua kama malipo ya Ibada zake, na ukihesabiwa ukubwa wa uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaeabudiwa basi kwa hakika Ibn Adam husika atadharau nakuona kua hakina thamani kila alichokifanya miongoni mwa Ibada zake mbele ya Mola wake hata kama ikwa amefanya kila kitu kwa ukamilifu, wachia mbali kasoro na uzembe ulio ndani yake Ibada hizo.

Hivyo Ibn Adam anatakiwa kuchukua tahadhari kubwa sana juu ya majukumu yake kwa Mola wake ili asije akaghafilika juu yake yake, na kutakiwa kua na khofu juu ya kuja kuadhibiwa kwake na anatakiwa awe ni mwenye kuzingatia maneno ya wenye Hikma na busara katika kutegemea msamaha wa Mola wake kwani kama Malaika Walioubwa kwa ajili ya Kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu watakua ni wenye kusema katika siku ya Malipo kua: 'Hakika sisi hatukukuabudu wewe Mola wetu ipasavyo' na hivyo Mtu anatakiwa awe na hali kama ya Khalilu Allah Ibrahim *Alayhi Salatu wa Salam* pale aliposema:

﴿ وَٱلَّذِيٓ أَطْمَعُ أَن يَغْفِرَ لِي خَطِيٓئَتِي يَوْمَ ٱلدِّينِ﴾

Waalladhee atmaAAu an yaghfira lee khatee-atee yawma alddeen.i(*Surat Ash-Shu'ara: 26:82)*

*Tafsir: **Na yeye (Allah Subhanah wa Ta'ala) ndie nnaemtumainia kua atanisamehee dhambi zangu katika siku ya Malipo.***

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua:

ما منكم من ينجيه عمله، قالوا: ولا أنت؟ قال: ولا أنا، إلا أن يتغمدني الله برحمته .

'Hakuna hata mmoja mingoni mwenu atakaeokoka kutokana na Amali zake katika Siku ya Malipo.' Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakauliza: 'Hata wewe *Ya Rasul Allah*?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: 'Naam, hata mie isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* atanifunika mimi kwa Rehma zake'** *(Sahih Bukhari na Muslim)*

2 - SUJUD AL SHUKR

❖❖❖❖

Sujud ya Kushukuru ambayo hua ni ya Sijda Moja tu ambayo hupendekezwa kuifanya pale unaponeemeshwa na Neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* au unapoepushwa na Hatari, Shari au madhara.

Na amesema Abu Bakrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Kila wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua kaipokea Habari nzuri basi alikua akisjudu kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala '***(ambapo hii ni hadithi iliyopokeleewa na Maimam Watano wakuu wa Hadith ambapo kwa upande wa Imam An Nasai na Imam At Tirmidhi basi wao wamesema kua hii ni Hadith Hasan Gharib)*

Na hivyo hii hua ni Sujud yenye kujitegemea peke yake yaani hutakiwi kuifanya wakati ukiwa ndani ya Sala kwani ukiifanya ndani ya Sala basi Sala yako hua ni Batil. Na ndani ya Sijda hii ambayo hua ni mara moja tu basi hua unatakiwa kusema mara 3 ndani yake maneno yafuatayo:

Subhana Rabbiya Al Aala wa bihamdihi

Au unaweza kusema maneno yafuatayo:

سجد وجهي للذي خلقه وصوره وشق سمعه وبصره بحوله وقوته.

اللهم اكتب لي بها عندك أجراً، واجعلها لي عندك ذخراً ، وضع عني بها وزراً، واقبلها مني كما تقبلتها من عبدك داود عليه السلام

Sajada Wajhi lilladhii Khalaqahu wa Sawwarahu, wa shaqqah samaahu, wabasharahu bi hawlihi wa Quwwatih Allahuma Uktub li biha ain-daka aAjran wa Daa anni biha wizran, Wajaalha li ain-daka Dhahran wa Taqabalha minni kama Taqabbalaha min Abdika Dauda*(Rawdat Al Talibin)*

*Tafsir: N**imesjudisha Uso wangu kwa Yule alieuumba na Kuupa Sura yake Uso huu, na akaupa uwezo wa Kuisikia na kuona kwa Utukufu na uwezo wake Ya Allah niandikie mimi malipo yangu mbele yako, na unirahisishie uzito kutokana nao, Ujaalie uwe ni hazina yangu ya Peponi na unikubalie kama ulivyomkubalia Mja wako Daud.***

Na pia unaweza kusema maneno yafuatayo mara 4 badala yake.

Subhana Allah wa Al Hamd lillahi wala illahaila Allahu Allahu Akbar hawla wala Quwwata Illa bi Allahi al A'liyyi Al Aadhiim

Na amesema Abd Rahman Ibn Awf *Radhi Allahu Anhu* kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alienda katika sehemu ambayo inahifadhiwa Sadaqah, na kisha akageukia upande wa Kibla na akasjudu, huku akiwa amebakia katika hali hio kwa mda mrefu, na kisha akanyanyua kichwa chake na kusema: 'Amenishukia mimi Jibril akiwa na habari njema, akaniambia kua: 'Yeyote yule atakaekusalia, basi na mimi nitamsalia na yeyote yule atakae kutumia Salam za kukutakia Amani basi na mimi nitamtumia Salam zangu za kumtakia Amani' hivyo na mimi nikasjudu kwa ajili ya kumshukuru*Allah Subhanah wa Ta'ala ''***(Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo anasema Mujtahid Imam Al Mundhiri Al Nishapuri kua: **'Hadith ya Shukr *yenye Sanad Sahih* ni ile hadith ya Al Baraa na ya Ka'ab Ibn Malik na wengineo.'**

Ambapo kuhusiana na Ka'ab Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* basi alikua ni yule Sahaba ambae alisilimua mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya kupewa habari njema ya kua amesamehewa Toba yake.

Na katika wakati wa kipindi cha Utawala wa *Amir Ul Muumnin* Abu bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu*baada ya kufariki ya kufariki *Rasul Allah Salallahuym Alayhi wa Salam,* na kutokea Mitume wa uongo akiwemo *Musallima Al Kadhab* ambaealisababisha madhara makubwa kwa Jeshi la Waislam lillopigana dhidi yake kutokana na kua na Jeshi kubwa lenye wafuasi waliouasi Uislam ambalo hata hivyo Jeshi lake lilishindwa baada ya kukabiliana na Jeshi la *Saifu Allah* Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu,* Na mwishowe Musalima kuuawa.

Hivyo baada ya *Amir Ul muumnin* Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* kupokea habari za Ushindi wa Jeshi hilo la Waislam na kuuawa kwa *Musallima Al Kadhab basi Amir Ul muumnin* Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* alisjudu kumshukuru*Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa ushindi huymo na kuuawa huko kwa Musallima.*(Imam Said Ibn Mansur)*

Ambapo anasema Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: **'Ama kuhusiana na Sijda ya Shukran basi hua inakubalika kuitekeleza kila unapopata kujaaliwa Neema mpya na *Allah Subhanah wa Ta'ala* , lakini hua haikubaliki Kwa Neema zinazoendelea, kwa sababu hua si zenye kusimama.'***(Al Majmuu)*

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam Zayn Ad Din Al Sunayki Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Masri Al Shafii basi anasema kua: **'Sijda ya Shukrani hua ni Sijda ambayo inapendekezwa kutekelezwa ppale zinapowasili habari nzuri au neema, kwa mfano kupatikana kwa Mtoto, Kupata heshima, kupata Mali, Kupatikana au kuwasili kwa Mtu aliepotea au ushindi dhidi ya maadui au pale inapopatikana Uokovu kutokana na kitu chenye Madhara au maangamizo kwa mfano kuepukana na Moto ambao ni wenye kusababisha vifo, kuepushwa na Kuzama kweye maji n.k.**

Na hii ni kutokana na msingi wa ile Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: 'Alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* kua: Nilimuomba mimi *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua anijaalie kua ni mwenye kuwaombea watu wa Ummah wangu, na akanikubalia kuwaombea sehemu tatu ya watu wa Umma wangu na hivyo nami nikasujudu kumshukuru Mola wangu.'

'Na kisha nikanyanyua kichwa changu na kumuomba*Allah Subhanah wa Ta'ala* kua anijaalie kua ni mwenye kuwaombea watu wa Ummah wangu, na akanikubalia kuwaombea sehemu tatu zaidi ya watu wa Umma wangu na hivyo nami nikasujudu kumshukuru Mola wangu.'

'Na kisha nikanyanyua kichwa changu tena na kumuomba*Allah Subhanah wa Ta'ala* kua anijaalie kua ni mwenye kuwaombea watu wa Ummah wangu, na akanikubalia kuwaombea sehemu nyengine tatu zaidi ya watu wa Umma wangu na hivyo nami nikasujudu kumshukuru Mola wangu.'

***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisjudu pia pale alipopokea barua kutoka Yemen kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* yenye habari za kusilimu kwa watu wa Hamdan.'**

‘Hivyo Sijda ya Shukran hua ni kwa ajili ya kushukurua kupatikana kwa Neema, kuepushwa na laana na mitihani na hua si kwa neema yenye muendelezo wa kila siku kama kua na Afya, kua na Imani ya Dini ya Kiislam, Kua huru na kutokana na kuhitajia misaada ya Watu n.k kwa sababu kama ikiwa Sijdat Shukr itatekelezwa kwa mambo hayo basi itakua ni wenye hali ya kua ni wenye kusjudu daima, na imetajwa Neema na Mitihani kwa sababu ni vitu vyenye kuonekana wazi.’

Na imenukuliwa kutoka kwa Imam Al Bayhaqi kua: ‘Inawezekana pia kusjudu kumshukuru *Allah Subhanah wa Ta’ala kwa* kupata usalama au kuepushwa baada ya kuona mtu ambae anafanya dhambi hadharani, kwa sababu Mtihani wa Dini hua ni mkubwa zaidi’

Ambapo kwa upande wa Imam Al Khwarizim ambae ni Mwanafunzi wa Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Farra Al Baghawi basi anasema kua: **‘Kuonesha Shukran kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* hua nibora zaidi kwa njia ya Kusali Sala ya Sunnah ya Rakaa mbili au kwa kutoa Sadaqah.’**

3-SIJDAT AL TILAWAH

❖❖❖❖

Sujud ya Kisomo cha Qur'an ambayo pia hujulikana kama Sajdah Al Tilawa.Ambayo hua ni Sujud inayotekelezwa na Muislam anapokua anasoma Qur'an na ndani yake akakutana na aya Maalum za Qur'an zenye kuzungumzia kuhusiana na Kusujudu.

Ambapo Sujud za aina hii hua ni Sujud za Sunnah inayotiliwa Mkazo sana na hivyo Msomaji wa Qur'an anapokutana na Aya husika basi haiangaliwi kama msomaji huyo yumo ndani ya Sala au nje ya Sala akiwa anasoma Qur'an tu kwani wakati ameisoma haya husika basi Msomaji hua ni mwenye kutakiwa Kusjudu.

Hivyo basi kama msomaji atakua yupo ndani ya Sala na akasoma aya husika basi akifikia sehemu ya Kusjudu basi atasjudu Sijda moja inayofanana Sijda ya Shukrani na kisha atakuja juu tena na kuendelea na kisomo chake.

Na kama Imam atakua ametekeleza Sunnah hio inayotiliwa mkazo basi na Maamuma pia hua na Wajibu wa kumfuata Imam wake na kutekeleza Sujud hio.

Ambapo amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua : **‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikuwa akisema katika kusujudu Sijda ya kisomo cha Qur’ani wakati wa usiku maneno yafuatayo**:

«سجد وجهي للذي خلقه وشق سمعه وبصره بحوله وقوته»

Na ndani yake Sijda hii yenye kusjudiwa kama Sijda ya Sala mara mbili basi hua unatakiwa kusema mara 3 ndani yake maneno yafuatayo:

Subhana Rabbiya Al Aala wa bihamdihi.

Kwani anasema *Mujaddid Ad Din* Imam Muhammad Idris Al Shafii katika Kitab Al Umm kua:**‘Na kama mtu akisema kama anavyosema katika Sijda ya Sala ya Kawaida basi hua inaruhusika na kama akibadilisha basi hua inaruhusika pia’**

Na kama alivyosema Imam Al Mutawwali kua: ‘**Hua ni Sunnah kuomba Dua baada ya kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kisha kuomba Dua katika Sijda hii kama vie ambavyo alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Usiku wa Miraj ambayo ni:**

سجد وجهي للذي خلقه وصوره وشق سمعه وبصره بحوله وقوته.

اللهم اكتب لي بها عندك أجراً، واجعلها لي عندك ذخراً ، وضع عني بها وزراً، واقبلها مني كما تقبلتها من عبدك داود عليه السلام

Sajada Wajhi lilladhii Khalaqahu wa Sawwarahu, wa shaqqah samaahu, wabasharahu bi hawlihi wa Quwwatih Allahuma Uktub li biha ain-daka aAjran wa Daa anni biha wizran, Wajaalha li ain-daka Dhahran wa Taqabalha minni kama Taqabbalaha min Abdika Dauda.(*Rawdat Al Talibin)*

*Tafsir:**Nimesjudisha Uso wangu kwa Yule alieuumba na Kuupa Sura yake Uso huu, na akaupa uwezo wa Kuisikia na kuona kwa Utukufu na uwezo wake Ya Allah niandikie mimi malipo yangu mbele yako, na unirahisishie uzito kutokana nao, Ujaalie uwe ni hazina yangu ya Peponi na unikubalie kama ulivyomkubalia Mja wako Daud.***

Na pia unaweza kusema maneno yafuatayo mara 4 badala yake.

سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ وَلاَ حَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ

Subhana Allah wa Al Hamd lillahi wala haila Allahu Allahu Akbar hawla wala Quwwata Illa bi Allahi al A'liyyi Al Aadhiim.

Utukufu ni wake Allah! Na Shukran ni zake Allah na hakuna Mungu isipokua Allah, Na Allah ndie Mkubwa zaid na Hakuna Nguvu wala Uwezo isipokua kutoka kwa Allah.

Ama kwa upande wa yule asiekua ndani ya sala na kua ni mwenye kusoma Qur'an na kisha akakutana na aya za Sujud Basi humbidi kufanya mambo yafuatayo:

Kutia nia ya Kufanya Sijda hio ya kisomo.

Kusema Allahu Akbar.

Kusjudu mara moja na kutamka Dhikr tulizozitaja.

Kuinuka kutoka kwenye Sijda na Kukaa kitako.

Kutoa Salam mara tu baada ya kukaa kitako.

Kuendelea na Kisomo chake.

Na amesema Abd Allah Ubn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitusomea Qur'an na hivyo akifika kwenye Aya ambayo ndani yake mmeamrishaa Sujud basi alikua akifanya Takbir na kisha Husjudu ambapo na sisi tulikua tukimfuata na kufanya hivyo hivyo'***(Sunan Abu Daud)*

Na akasema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua:

***Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* alisoma Surat An Najm wakati akiwa Makkah na akasjudu wakati alipokua akiisoma na hivyo wote waliokua pamoja nae wakasjudu isipokua mtu mzima mzee mmoja ambae yeye aliokota gao la Kokoto au Mchanga na kulinyanyua hadi kwenye paji lake la uso (na kujigusisha nalo kwenye paji la uso) na kusema: Hili litajitosheleza mimi, na baadae nikamuona mimi Mzee huyo akifariki huku akiwa Kafiri.'** *(Sahih Muslim)*

Na akasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Wakati Ibn Adam anaposoma Aya ya Kusjudu na kisha akasjudu, basi Shaytani**

hukimbia huku akiwa analia na kusema: 'Ole wangu Mimi kwani Ibn Adam ameamrishwa Kusjudu na amesjudu hivyo atakua ni mwenye kuingia Peponi, nami niliamrishwa Kusjudu nikakataa na nitaingia Motoni''*(Sahih Muslim)*

Na hapa inabidi tufahamiane kidogo hapa kwenye Sijda ya Kisomo kwa kuambiana kua inapotokea pale Mtu yuko ndani ya Sala na kisha akasoma aya yenye Sijda basi akienda chini Kusjudu lazima kwanza aseme *Allahu Akbar,*huku akiwa ni mwenye kunyanyua mikono yake hadi katika usawa wa masikio kama kwenye *Takbir al Ihram*na pia akitoka kwenye Sijda kuja juu kuendelea na kisomo basi lazima aseme*Allahu Akbar*huku akiwa ni mwenye kunyanyua juu mikono pia na kisha ndio aendelee na kisomo cha ndani ya Sala.

Lakini kama akiwa hayuko ndani ya Sala labda tuseme amekaa kitako wakati akiisoma aya husika basi atasema *Allahu Akbar*bila ya kunyanyua mikono wakati akienda kwenye Sujud na akija juu atatoa Salam na kuendelea na kisomo.

Na Sijda ya Kisomo hua Si Sijda ya Fardhi bali ni Sijda ya Sunnah Muakkadah yaani Sunnah inayotiliwa mkazo,na hii ni kulingana na hadith isemayo: '**Amesema Rabiah*Radhi Allahu Anhu* kua: Umar Ibn Al Khattab *RadhiAllahu Anhu* alisoma Surat An Nahl katika Siku ya Ijumaa wakati akiwa Juu ya Mimbar. Na alipofikia aya ya Kusjudu iliyomo ndani yake basi akashuka kutoka kwenye Mimbar na kisha Akasjudu na hivyo Watu nao Wakasjudu.**

Na kisha katika Ijumaa iliyofuatia Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasoma tena Surat An Najm Juu ya Mimbar.

Na alipofika kwenye aya ya Sujud basi akasema: Enyi Watu tunaposoma Aya za Sajda (katika Khutba nje ya Sala) basi atakaesujudu atakua amefanya Jambo Sahih Lakini hapo hapo hakuna makosa kwa yeyote yule ambae hatosjudu.

Rabiah*Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: **'Na katika Ijumaa hio baada ya kusema maneno hayo basi Umar *Radhi Allahu Anhu* Hakusjudu na akasema Allah Hakuifanya Sujud ya Kisomo cha Aya kua ni Lazima, lakini kama tukipenda na kutaka basi tunaweza kusjudu.'** *(Imam Bukhari)*

Kwa maana hio basi hapa inabidi tufahamiane tena kua ikiwa kisomo kiko nje ya Sala, labda kwenye Darsa au Khutba na Imam anaesoma akasjudu basi Wanaomsikiliza hua hawana ulazima wa kusjudu, ila hua ni bora kwao kusjudu.

Na pia kama Imam anasalisha na kuna mtu ambae yeye ameshasali hapo kabla na anamsikia Imam huyo katika kisomo chake hicho na kisha Imam huyo akasoma aya yenye kumtaka kusjudu na hivyo akasjudu ndani ya Sala na Maamuma wake nao wakasjudu, basi yule anaesikia wakati hayumo ndani ya Sala ya jamaa hio basi hua hatakiwi kusjudu, kwa sababu kisomo hicho ni cha ndani ya Sala.

Kwani kuna Hadithnyengine zinazosema kuwa Mtume *Salallahu Alayhi wa Salam* hakusujudu katika Aya ya Sajda kama katika Hadithi iliyopokewa na Zaid Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu,* ambae amesema: '**Mimi niliwahi kusoma Surat Al Najm mbele ya *RasulAllah Salallahu Alayhi wa Salam,* lakini hakusjudu kutokana nayo.***'(Imam Al Bukhari)*

Lakini kama ikiwa ndani ya Sala na Imam kasoma Aya ya Sujud na akasjudu basi na Maamuma humbidi kusjudu pia kumfuata Imam wake, kama vile ambavyo Utakapomkuta Imam anasoma Qunut baada ya Rukuu labda katika Sala Al Maghrib au Ishaa n.k basi na wewe hutakiwi kuenda kwenye sijda bali hukibidi kuitikia Dua hio ya Qunut kwanza kuenda sambamba na Imam wako katika kukamilisha Sala yako ya Jamaa.

Shaykh Ul Islami Imam Zayn Ad Din Al Sunayki Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Masri Al Shafii anasema kua: '**Amesema Abd Rahman Ibn Awf *Radh Allahu Anhu* kua: 'Nilimuona Mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisjudu mara 10 katika aya isemayo:''**

﴿إِذَا ٱلسَّمَآءُ ٱنشَقَّتْ﴾

I<u>dha</u> alssam<u>a</u>o inshaqqat*(Surat Al Inshiqaq 84:1)*

*Tafsir**: Wakati Mbingu zitakapopasuka Mbingu.***

Ambapo hii ni hadith iliyonukuliwa na Imam Al Bazar.

Na hakuna Sunnah ya Kusjudu katika kusikia au kusoma aya yenye Sijda pale inapokua Mtu husika hayuko Tohara au yuko katika hali ya kua ni mwenye kulewa. Kwa sababu hua ni haramu kwao wao, ambapo kwa upande wa Imam Jamal Ad Din Abu Muhamamd Abd Al Rahim Ibn Al Hasan Al Umawi Al Qurashi Al Asnawi Al Shafii Al Misri basi amesema kua: 'Hakuna Sijda ya Kisomo kwa yule mtu ambae hajatilia umakini kisomo husika au kwa aliekua katika hali ya kua usingizini kwa sababu hawakua na nia ya kusikiliza kisomo husika.'

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Bahadir Al Zarkashi basi yeye anasema kua**: 'Hua ni wajibu Kusjudu kwa Mtu anaesali na akazisomaAya za Qur'an zenye kutakiwa kusjudu.'**

Na *Sijdat At Tilawah* hua ni kwa ajili ya yule anaesikiliza Qur'an na wala si kwa yule anaesikia kisomo cha Aya husika, kama anavyosema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Kusjudu hua ni Wajibu kwa yule Mtu aliekua na nia ya kusikiliza Kisomo husika'** na pia amesema Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Kusjudu hua ni wajibu kwa mtu aliekusudia kusikiliza kisomo husika.'***(Imam Al Bayhaqi)*

Na kama ikiwa Mtu anasali na kisha akasoma aya za Qur'an zenye kumtaka kusujudu lakini akajikuta kua anarukuu badala yake lakini hapo hapo akakumbuka kua anatakiwa Asjudu basi Mtu huyo hua haruhusiwi tena kusjudu Sijda ya Kisomo kwa sababu katika hali kama hii basi mtu huyo hua tayari ameshaingia kwenye Nguzo ya Sala ambayo ni ya Rukuu, na hivyo hua hawezi kukatisha Fardhi kwa ajili ya Sunna, lakini kama ikiwa hajaingia kwenye hatua ya kurukuu basi hua anaruhusika kusjudu, na pia kama ikiwa amesoma aya husika na kisha akaelekea kwenye kusujudu lakini lakini akaona kua bora asisjudu na akarudi tena juu katika kisimamo basi hua hamna tatizo kwa sababu Sijda hii ni Sunnah na si Fardhi .

Kwani kama alivyosema Imam Abu Al Qasim Abd Al Karim Ibn Muhammad Ibn Abd Al Karim Ibn Fadhl Ibn Hasan Al Rafii Al Qazwini Al Shafii kua: ***'Sijdat Al Tilawah* ni Sunnah' basi Mtu husika hua anayo haki ya kuikatisha kama vile alivyokua anayo haki ya kutoitekeleza.Na ukamilifu wake ni kutosoma baada yake.'**

Na anasema Imam Al Bulqini kua**: 'Kama ilivyokua haitakiwi kusali katika baadhi ya Nyakati isipokua kwa sababu maalum inayokubalika, basi ndio vile vile pia ambavyo haikubaliki kuisoma Aya husika kwa ajili ya kusjudu tu, kwa sababu hii hua ni kuchagua sababu ya kusujudia katika nyakati ambazo haziruhusiki.'**

AYA ZA SIJDA NDANI YA QUR'AN

❖❖❖

Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Aya za Kusjudu zilizomo ndani ya Qur'an kwani kuna wasemao kua ni Aya 14 na kuna wasemao kua ni aya 15. Ambazo aya zote hizo kama ukizisoma na kuzifahamu maana yake na kutafakkari basi bila ya shaka utasjudu tu baada ya kuzisma kwake, na hizo ni aya zifuatazo:

1-Surat Al Araf 7:206

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ عِندَرَبِّكَ لاَيَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ وَيُسَبِّحُونَهُ وَلَهُ يَسْجُدُونَ﴾

Inna alladheena AAinda rabbika la yastakbiroona AAan AAibadatihi wayusabbihoonahu walahu yasjudoona.*(Surat Al Araf 7:206)*

*Tafsir:**Kwa hakika wale ambao waliokua na Mola wako (Malaika wake)kamwe hawakua ni wenye kujiona katika kutekeleza Ibada zao kwake, bali ni wenye kumtukuza kwa sifa zake na ni wenye kumsujudia.***

2-Surat Ar Rad 13:15

﴿وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَن فِي ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ طَوْعاً وَكَرْهاً وَظِلالُهُم بِٱلْغُدُوِّ وَٱلآصَالِ﴾

Walillahi yasjudu man fee alssamawati waAl ardhi tawAAan wakarhan wadhilaluhum bialghuduwwi waAl asali*(Surat Ar Rad 13:15)*

*Tafsir: **Na kwake yeye Allah (Subhanah wa Ta'ala)pekee ndiko kunakosjudiwa na kila kilichomo Mbinguni na Ardhini kitake kisitae na pia ndi vifanyavyo vivuli vyao Asubuhi na Jioni.***

3-Surat An Nahl 16:49

﴿وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَا فِي ٱلأَرْضِ مِن دَآبَّةٍ وَٱلْمَلآئِكَةُ وَهُمْ لاَ يَسْتَكْبِرُونَ﴾

Walillahi yasjudu ma fee alssamawati wama fee Al ardhi min dabbatin waalmala-ikatu wahum la yastakbiroona*(Surat An Nahl 16:49)*

*Tafsir: **Na kwake yeye Allah (Subhanah wa Ta'ala) ndiko kunakosujudiwa na kila kilichomo Mbinguni na Ardhini miongoni mwa Viumbe wenye mienendo mbali mbali na Malaika, na wala si wenye kufanya kiburi.***

4-Surat Al Isra 17:107

﴿قُلْ آمِنُواْ بِهِ أَوْ لاَ تُؤْمِنُوَاْ إِنَّ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْعِلْمَ مِن قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلأَذْقَانِ سُجَّداً﴾

Qul aminoo bihi aw la tu/minoo inna alladheena ootoo alAAilma min qablihi idha yutla AAalayhim yakhirroona lil-adhqani sujjadan*(Surat Al Isra 17:107)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi Wa Salam kuwaambia Makafiri) Iwe mnaimini (Hii Qur'an) au hamuiamini, basi kwa hakika wale waliopewa Ilm kabla yake, wanaposomewa Qur'an hua ni wenye kuangakia Nyuso zao katika kusjudu kwa unyenyekevu.***

5-Surat Maryam 19:58

﴿أُولَٰئِكَ ٱلَّذِينَ أَنْعَمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِم مِّنَ ٱلنَّبِيِّيْنَ مِن ذُرِّيَّةِ ءادَمَ وَمِمَّنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ وَمِن ذُرِّيَّةِ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْرَائِيلَ وَمِمَّنْ هَدَيْنَا وَٱجْتَبَيْنَآ إِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُ ٱلرَّحْمَٰنِ خَرُّواْ سُجَّداً وَبُكِيّاً﴾

Ola-ika alladheena anAAama Allahu AAalayhim mina alnnabiyyeena min dhurriyyati adama wamimman hamalna maAAa noohin wamin dhurriyyati ibraheema wa-isra-eela wamimman hadayna waijtabayna idha tutla AAalayhim ayatu alrrahmani kharroo sujjadan wabukiyyan*(Surat Maryam 19:58)*

Tafsir: ***Wao nido wale ambao Allah (Subhanah wa Ta'ala) amewaneemesha miongoni mwa Manabii kutoka katika kiza cha Adam na wale ambao tuliwabeba (kwenye Meli)pamoja na Nuh na kizazi cha Ibrahim na Israil na wale tuliowaongoza mongoni mwa tuliowachagua. Wanaposomewa juu yao aya zetu basi hua ni nwenye kusujudu na kulia.***

6-Surat Al Hajj 22:18

﴿أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَن فِي ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَن فِي ٱلأَرْضِ وَٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ وَٱلنُّجُومُ وَٱلْجِبَالُ وَٱلشَّجَرُ وَٱلدَّوَآبُّ وَكَثِيرٌ مِّنَ ٱلنَّاسِ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ ٱلْعَذَابُ وَمَن يُهِنِ ٱللَّهُ فَمَا لَهُ مِن مُّكْرِمٍ إِنَّ ٱللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَآءُ﴾

Alam tara anna Allaha yasjudu lahu man fee alssamawati waman fee Al ardhi waalshshamsu waalqamaru waalnnujoomu waaljibalu waalshshajaru waalddawabbu wakatheerun mina alnnasi wakatheerun haqqa AAalayhi alAAadhabu waman yuhini Allahu fama lahu min mukrimin inna Allaha yafAAalu ma yasha/o.*(Surat Al Hajj 22:18)*

*Tafsir:****Hivi hamuoni nyinyi kua kwake yeye Allah (Subhanah wa Ta'ala) ndiko kunakosujudiwa na kila kilichomo Mbinguni na Ardhini, na kwenye Jua na kwenye Mwezi na kwenye Nyota na kwenye Milima na Miti na Viumbe hai na wengie mingoni mwa watu? Na hivyo kuna wengi miongoni mwa Watu wanaostahiki Adhabu, na yeyote yule atakaedhalilishwa na Allah (Subhanah wa Ta'ala) basi hakuna atakaeweza kumheshimisha. Kwa hakika Allah ni mwenye kufanya kile akitakacho.***

7-Surat Al Hajj 22:77

﴿أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ ٱرْكَعُواْ وَٱسْجُدُواْ وَاعْبُدُواْ رَبَّكُمْ وَٱفْعَلُواْ ٱلْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Hajj 22:77)*

Tafsir: ***Enyi wale ambao Mlioamini, Rukuuni na Sujuduni na Muabuduni Mola wenu na fanyeni Mema ili mpate kua ni wenye Kufaulu.***

8-Surat Al Furqan 25:60

﴿وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ ٱسْجُدُواْ لِلرَّحْمَٰنِ قَالُواْ وَمَا ٱلرَّحْمَٰنُ أَنَسْجُدُ لِمَا تَأْمُرُنَا وَزَادَهُمْ نُفُوراً﴾

Wa-idha qeela lahumu osjudoo lilrrahmani qaloo wama alrrahmanu anasjudu lima ta/muruna wazadahum nufooran*(Surat Al Furqan 25:60)*

*Tafsir: **Na wanapoambiwa: 'Msujudieni Mwingi wa Rehma (Allah (Subhanah wa Ta'ala))' basi hua ni wenye kusema: 'Na ndio nani huyo mwingi wa Rehma? Hivi unatutaka (Ewe Muhammad) tusujudie kile ambacho unatuamrishia' na haiwazidishii kitu isipokua upotovu.***

9-Surat An Naml 27:25

﴿أَلاَّ يَسْجُدُواْ لِلَّهِ ٱلَّذِى يُخْرِجُ ٱلْخَبْءَ فِى ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ﴾

Alla yasjudoo lillahi alladhee yukhriju alkhabaa fee alssamawati waAl ardhi wayaAAlamu ma tukhfoona wama tuAAlinoona*(Surat An Naml 27:25)*

*Tafsir**: Al La(Neno hili lina maana mbili kwanza ni kua Shaytan amewazuia kutokana na njia sahih ya Allah (Subhanah wa Ta'ala) ili wasiweze kumuabudu, na pili ni kua ili wapate kuweza kumuabudu Allah (Subhanah wa Ta'ala)) ni Allah (Subhanah wa Ta'ala)ndie anaedhidhirisha kilichofichikana Mbinguni na Ardhini na ni mwenye kujua kila mnachokificha na kila mnachokiweza wazi.***

10-Surat As Sajda 32:15

﴿إِنَّمَا يُؤْمِنُ بِآيَاتِنَا ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِّرُواْ بِهَا خَرُّواْ سُجَّداً وَسَبَّحُواْ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ لاَ يَسْتَكْبِرُونَ﴾

Innama yu/minu bi-ayatina alladheena idhadhukkiroo biha kharroo sujjadan wasabbahoo bihamdi rabbihim wahum la yastakbiroona*(Surat As Sajda 32:15)*

*Tafsiri: **Ni wale tu wenye kuamini Aya zetu ndio ambao wanapokumbushiwa juu yake hua ni wenye wenye kuanguka chini na kusjudu na kumtukuza kwa sifa zake Mola wao (Allah Subhanah wa Ta'ala) na wala hawajioni.***

11-Surat Fusilat 41:37

﴿وَمِنْ آيَاتِهِ ٱللَّيْلُ وَٱلنَّهَارُ وَٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ لاَ تَسْجُدُواْ لِلشَّمْسِ وَلاَ لِلْقَمَرِ وَٱسْجُدُواْ لِلَّهِ ٱلَّذِى خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ﴾

Wamin ayatihi allaylu waalnnaharu waalshshamsu waalqamaru la tasjudoo lilshshamsi wala lilqamari waosjudoo lillahi aladhee khalaqahunna in kuntum iyyahu taAAbudoona*(-Surat Fusilat 41:37)*

*Tafsir: **Na katika Aya zake Ni Usiku na Mchana na Juan a Mwezi, hivyo Msisujudie Jua wala mwezi bali MsujudieniAllah (Subhanah wa Ta'ala) Alieziumba kama kweli nyinyi Mnamuabudu yeye.***

12-Surat An Najm 53:62

﴿فَٱسْجُدُواْ لِلَّهِ وَٱعْبُدُواْ﴾

Faosjudoo lillahi waoAAbudoo(Surat An Najm 53:62)

Tafsir: ***Hivyo Angukeni kumsujudia Allah (Subhanah wa Ta'ala) na kumuabudu.***

13-Surat Al Inshiqaq 84:21

﴿وَإِذَا قُرِىءَ عَلَيْهِمُ ٱلْقُرْآنُ لاَ يَسْجُدُونَ﴾

Wa-idha quri-a AAalayhimu alqur-anu la yasjudoona*(Surat Al Inshiqaq 84:21)*

Tafsiri: ***Na anaposomewa juu yao Qur'an hawasjudu.***

14-Surat Al Alaq 96:19

﴿كَلاَّ لاَ تُطِعْهُ وَٱسْجُدْ وَٱقْتَرِب﴾

Kalla la tutiAAhu waosjud waiqtarib*(Surat Al Alaq 96:19)*

Tafsir: ***La (Ewe Muhammad Salallahuym Alayhi wa Salam) Usimtii (Abu Jahl), Bali Msujudie Allah (Subhanah wa Ta'ala) Na umkaribie.***

Kutoka kwa Abu Huraira, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alisujudu katika "Mbingu ilipopasuka" na usome kwa jina la Mola wako Mlezi.

Na aya ya 15 ni ayaambayo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua hii ni aya yenye Sijda ya Shukran ndani yake.Kwani aya hio ni ile aya inayofuata baada ya aya inayozungumzia wabirukaji Ukuta waliobirukia ndani ya Chumba cha Nabii Daud kwa ajili ya kutaka kutatuliwa kesi yao kwa kusema:

﴿إِنَّ هَذَآ أَخِى لَهُ تِسْعٌ وَتِسْعُونَ نَعْجَةً وَلِىَ نَعْجَةٌ وَاحِدَةٌ فَقَالَ أَكْفِلْنِيهَا وَعَزَّنِى فِى ٱلْخِطَابِ﴾

Inna hadha akhee lahu tisAAun watisAAoona naAAjatan waliya naAAjatun wahidatun faqala akfilneeha waAAazzanee fee alkhitabi*(Surat Sad 38:23)*

Tafsir: ***Hakika Huyu Ndugu yangu anao Tisini na Tisa Majike wa Kondoo Na Mimi nna Kondoo Jike Mmoja tu Lakini Ananiambie Nipe Kondoo wako(Huyo Mmoja ili wangu watimie 100) Na Amenizidi Nguvu.***

Ambapo *Allah Subhanah waTa'ala* anaelezea lile lilofuatia baada ya Nabii Daud kupewa kesi hio,katika aya ambayo ambayo inasema

﴿ قَالَ لَقَدْ ظَلَمَكَ بِسُؤَالِ نَعْجَتِكَ إِلَىٰ نِعَاجِهِ وَإِنَّ كَثِيراً مِّنَ ٱلْخُلَطَآءِ لَيَبْغِي بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ إِلاَّ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّالِحَاتِ وَقَلِيلٌ مَّا هُمْ وَظَنَّ دَاوُودُ أَنَّمَا فَتَنَّاهُ فَٱسْتَغْفَرَ رَبَّهُ وَخَرَّ رَاكِعاً وَأَنَابَ﴾

Qala laqad *dh*alamaka bisu-ali naAAjatika ila niAAajihi wa-inna katheeran mina alkhulata-i layabghee baAAduhum AAala baAAdin illa alladheena amanoo waAAamiloo alssalihati waqaleelun ma hum wa*dh*anna dawoodu annama fatannahu faistaghfara rabbahu wakharra rakiAAan waanaba.*(*Surat Sad 38:24)*

*Tafsir:**Akasema (Nabii Daud) kwa Hakika Amekudhulumu Katika Kumtaka Kondoo wako Na kwa Hakika wengi Miongoni mwa Washirkka Wanadhulumiana Baadhi yao Miongoni mwa Baadhi yao Isipokua wale Walioamini Na Wakafanya Mema Na hao Ni Wachache miongoni mwao Na Akagundua Daudi Kua kwa Hakika Tumemjaribu Hivyo amaomba Msamaha kwa Mola wake Na Akaanguka chini na Kurukuu na kusjudu akitubu.***

Hii ndio aya ambayo Wanazuoni wametofautiana kama ni ya Sijda ama la, kwani amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua**: 'Nimemuona mimi*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akisjudu kwa Sura Sad..Hii sio Sijda ya Kisomo'***(Imam Bukhari)*

Ambapo amesema Abu Said Al Khudr *Radhi Allahu Anhu kua:* ***Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam* alituhutubia sisi na kisha akasoma aya ambayo ndaniyake ilikua ina Sijda, hivyo nasi tukasimama kujitayarisha Kusjudu, na alipotuona kua tuko katika hali hio basi *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* akasema: 'Mmejitarayarisha Kusujudu wakati Hii ni Toba ya Mtume.' Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* akashukuka na kusjudu.***'(Imam Abu Daud)*

Hivyo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hii ni Sijda ya Shukrani kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* baada ya Nabii Daud kukubaliwa Toba yake, na inapendekezwa kusujudiwa nje ya Sala, yaani baada ya kumaliza Sala, na hairuhusiki kuisjudu ndani ya Sala, kwani ikisjudiwa ndani ya Sala iwe kwa kusahau au kwa kutojua basi hua ni yenye kuibatilisha Sala husika, na hivyo Mtu atakaesjudu ndani ya Sala kutokana nayo basi hua anatakiwa asjudu *Sijdat Sahw* baada yake.'*(Al Mughni Al Muhtaj)*

Ama kwa upande mwengine basi kuna Wanazuoni wanaosema kua hii ni Sijda ya Kisomo, na huo na Mtizamo wa Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Abd Allah Ibn Mubarak,Imam Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Muhammad Ibn Is-haq.

Na hapa inabidi tufahamiane kua ingawa tunaona kua huu ni Mtizamo wa Imama Muyhmammad Idris Al Shafii, lakini si Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, kwa sababu Kwa kila Madhhab basi Wanazuoni wake hua wanashikamana na Mitizamo ya wengi miongoni mwa Wanazuoni wenye sifa ya Kua na Uwezo wa Kutoa Hukmu kwenye vyanzo vya Fiqh yaani Qur'an, Sunna na Makubaliano ya Ijmaa katika Madhhab husika, hivyo basi kama mtizamo wa Imam mkuu wa Madhhab utakua unapingana na mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab husika basi mtizamo wa Imam Mkuu hua haupewi kipaumbele. Na hivyo utakaofuatwa na kutegemewa na Madhhab husika hua ni mtizamo wa waliokubaliana nao Wanazuoni hao wa Madhhab husika.

Kwa maelezo zaidi basi soma kitabu changu cha Ijihad na Taqlid, Historia ya Wanazuoni na Madhhab yao Katika Uislam ambamo ndani yake nimeelezea kwa kina juu ya jambo hili.

Ama Tunapoziangalia Aya hizi za Kisomo chenye kutakiwa kuleta Sijda ndani ya Qur'an tunaona kua Surat Al Hajj imebarikiwa kua na Sijdat Tilawah mbili nadani yake ambazo ni katika aya zifuatazo:

Aya isemayo:

﴿أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَن فِي ٱلسَّمَاوَاتِ وَمَن فِي ٱلأَرْضِ وَٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ وَٱلنُّجُومُ وَٱلْجِبَالُ وَٱلشَّجَرُ وَٱلدَّوَآبُّ وَكَثِيرٌ مِّنَ ٱلنَّاسِ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ ٱلْعَذَابُ وَمَن يُهِنِ ٱللَّهُ فَمَا لَهُ مِن مُّكْرِمٍ إِنَّ ٱللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَآءُ﴾

Alam tara anna Allaha yasjudu lahu man fee alssamawati waman fee Al ardhi waalshshamsu waalqamaru waalnnujoomu waaljibalu waalshshajaru waalddawabbu wakatheerun mina alnnasi wakatheerun haqqa AAalayhi alAAadhabu waman yuhini Allahu fama lahu min mukrimin inna Allaha yafAAalu ma yasha/o*(Surat Al Hajj 22:18)*

*Tafsir:**Hivi hamuoni nyinyi kua kwake yeye Allah (Subhanah wa Ta'ala) ndiko kunakosujudiwa na kila kilichomo Mbinguni na Ardhini, na kwenye Jua na kwenye Mwezi na kwenye Nyota na kwenye Milima na Miti na Viumbe hai na wengie mingoni mwa watu? Na hivyo kuna wengi miongoni mwa Watu wanaostahiki Adhabu, na yeyote yule atakaedhalilishwa na Allah (Subhanah wa Ta'ala) basi hakuna atakaeweza kumheshimisha. Kwa hakika Allah ni mwenye kufanya kile akitakacho.***

Na aya isemayo:

﴿أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ ٱرْكَعُواْ وَٱسْجُدُواْ وَاعْبُدُواْ رَبَّكُمْ وَٱفْعَلُواْ ٱلْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Hajj 22:77)*

*Tafsir: **Enyi wale ambao Mlioamini, Rukuuni na Sujuduni na Muabuduni Mola wenu na fanyeni Mema ili mpate kua ni wenye Kufaulu.***

Ambapo kwa Upande wa Wafuasi wa Madhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: '**Kama ilivyosema Hadith iliyomo katika Sunana Imam Abu Daud isemayo kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Surat Al Hajj imependelewa zaidi ya Sura nyeingie kwa kua na Sijda mbili ndani yake, hivyo mtu yeyote Yule asieleta Sijda mbili ndani yake basi bora asizisome aya hizo''** ambapo kwa upande wa Imam Al Tirmidhii amesema kua hii si Hadith Sahih.

Hivyo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wanasema kuhusiana na aya ya pili miongoni mwa aya hizi za Surat Al Hajj ambayo ni hii isemayo:

﴿أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ ٱرْكَعُواْ وَٱسْجُدُواْ وَاعْبُدُواْ رَبَّكُمْ وَٱفْعَلُواْ ٱلْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Hajj 22:77)*

*Tafsir: **Enyi wale ambao Mlioamini, Rukuuni na Sujuduni na Muabuduni Mola wenu na fanyeni Mema ili mpate kua ni wenye Kufaulu***

Kwani anasema Jarrah Allah Sultan Al Balagha Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kua: **'Kila mara wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapozungumzia Rukuu na Sujudu pamoja katika Aya basi Sijda inayozungumziwa ndani yake aya hio hua ni Sijda ya Sala na haiiwi ni Sijda ya Tilawah(ya kisomo) na hii ni kama vile pale aliposema *Allah Subhana wa Ta'ala* katikaSurat Al Imran katika aya ifuatayo:'**

﴿ يَٰمَرۡيَمُ ٱقۡنُتِي لِرَبِّكِ وَٱسۡجُدِي وَٱرۡكَعِي مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ ﴾

Ya Maryamu uqnutee lirabbiki waosjudee wairkaAAee maAAa alrrakiAAeena*(Surat Al Imran 3:43)*

Tafsir: ***Ewe Maryam simama kwa ajili ya Mola wako na Usujudu, na kua miongoni mwa wenye Kurukuu.***

Ambayo haihitaji Kurukuu baada ya kuisoma kwake.

Na anasema Shaykh U Islami Imam Zakarriyah Al Ansari Kua: **'Kama Mtu ataleta Sijdat Tilawat kaba ya kumaliza aya yenye kutakiwa kuleta Sijdat Tilawat basi sijda hio hua haihesabiki, hata kama itakua kabla ya kumaliza herufi moja, na hii ni kwa sababu amesujudu kabla ya kufikia wakati wake na mahali pake.'**(*Asna Matalib)*

HUKMU ZA SIJDAT AT TILAWAH

❖❖❖

Miongoni mwa Hukmu za Sijda ya Kisomo ni kua: '**Mtu anaefanya Sijda hio anatakiwa awe Tohara, ambapo kila kinachobatilisha Sala basi hubatilisha pia Sijda hii na awe ni mwenye kuelekea Kibla katika Wakati wa Kufanya Sijda hio.**

Hua ni Sunna Kusjudu pale inaposikikana Aya ya Kusjudu inaposomwa hata kama msomaji atakua ni Mtoto mdogo.

Kama moja kati ya Aya za kisomo ikisomwa na Mlevi, mwendawazimu au mtu asiekua Tohara,basi kwa wale watakaosikia hawatoruhusika kusjudu hata kama watapenda na hata kama ni Sunna na hii ni kwa Sababu, Quran hua hairuhuikia kusomwa na watu kama hao.

Kama mwanamke akiwa hayuko Tohara labda yuko katika siku zake n.k na kisha akasoma Moja kati ya aya hizo kwa Moyo basi nae haruhusiki Kusjudu hata kama atataka kutekeleza Sunnah hio.

Ili Utekeleze Sunnah hii inayopendekezwa ya kusujudu pale inaposomwa moja kati ya Aya hizi basi hukubidi kua Unajua kua hii ni aya ya Kusjudu, au umeona kua Imam Ameenda Chini na kujua kua hii ni Aya ya Kusjudu, hivyo kama uko peke yako na hujui kua ni aya ya Kusjudu basi haina haja Kusjudu.

Ama kwa wale wasiojua na watataka kufuatilia basi Siku hizi Kuna Misahafu ambayo ndani yake katika kila aya yenye Neno Sujud ambalo limepigiwa Mstari, hivyo hii hua ni alama inayoonesha kua ukiisoma aya husika basi hua unatakiwa Usjudu.

Kwa mtu aliekua ndani ya Sala basi ili asjudu hua inambidi awe ni Mwenye kuisoma yeye mwenyewe aya hio ya Kusjudu au Isomwe na Imam wake Kwa maana hio basi hua haitakiwi Kusjudu kwa mtu aliemo ndani ya Sala na kisha akamsikia Mtu aliekua anasoma Qur'an labda Msikitini na akaisoma Aya ya Kusjudu.

Na hii ni kwa Sababu Kisomo alichokisikia yeye hakimo ndani ya Sala yake na wala hakihusiani na Ibada ya Sala yake, na hivyo akisjudu kutokana na kisomo hicho cha mtu aliekua nje ya Sala basi Sala ya Aliesjudu hubatilika.

Na Miongoni mwa Hukmu zake pia ni kua:

Hairuhusiki Kuchagua Kisomo cha Aya ya Sijda peke yake wakati ukiwa kwenye Sala ili upate Malipo ya Sunnah ya kusjudu Ndani yake, ambapo hata hivyo Hukmu hii haijumuishi Sala ya Ijumaa kwani ndani ya Sala ya Ijumaa hua inakubalika kufanya Hivyo kwani hua ni SunnaIngawa Hadith ya *Amir Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* inasema kua ni Sunna Kusjudu kwa Msomaji Khutba ya Ijumaa atakaesoma Aya ya Kusjudu kama atataka na Maamuma wanaweza wakasjudu kama Watataka kumfuata Khatib lakini kwa Upande Wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kua Kama Khatib atasoma aya Ya Kusjudu Juu ya Mimbar basi yeye itambidi Asjudu.

Lakini kwa Wanaomsikiliza hawato ruhusika kusjudukwani Hairuhusiki na inachukiza Kusoma kwa makusudi Aya za Kusjudu katika Nyakati ambazo tatu za Siku ambazo hairuhusiki KusjuduNyakati hizo ni pale Jua linapochomoza, Jua linapokua Katikati Juu ya Utosi na Jua linapozama, na hii ni kwa Sababu ya kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amevipanga vipindi vya saa za Sala tano katika hali ya kua visiende sambamba na Nyakati walizokua wakifanya Ibada zao watu wanaoabudu Jua.

Hivyo kwa wale wanaoabudu Jua hua ni wenye Kusjudu katika Nyakati hizo tatu, na hivyo kwa Muislam Kusali au kusjudu katika Nyakati hizo bila dharurra inayokubalika hua hakufai kwani hua ni kujishabihisha na Wanaoabudu Jua.

Kwa anaesali na akasoma aya yenye Sujud ndani yake na akasjudu basi Haitakiwi kuwe na Muda mrefu baina ya Sijda ya kisomo hicho na sijda ya Sala husika Kama ikiwa Mtu anataka kutekeleza Sunnah hii ya Aya ya Kusjudu lakini ikawa hawezi labda kutokana na kua Hana Udhu, au Anaumwa au yuko katika sehemu ambayo si Tohara na hawezikusjudu juu yake basi anaweza kufanya Dhikr ifuatayo mara 4 badala yake:

سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ وَلاَ حَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ

Subhana Allah wa Al Hamd lillahi wala illahaila Allahu Allahu Akbar hawla wala Quwwata Illa bi Allahi al A'liyyi Al Aadhiim.

Yaani **Utukufu ni wake Allah! Na Shukran ni zake Allah na hakuna Mungu isipokua Allah, Na Allah ndie Mkubwa zaid na Hakuna Nguvu wala Uwezo isipokua kutoka kwa Allah.**

Na pia, kwa Sijda ya kisomo kinachofanywa nje ya Salah h, hua kuna masharti mawili, nayo ni:

Sharti la Kwanza: Kurudiwa kwa aya moja ya Sajadah mara kadhaa katika kisomo kimoja.

Katika hali hii inatosha kwa mwenye kuisikia na kuisoma aya hii kwa kuitekeleza kuisjudu sijda mara moja tu, hivyo hata ikirudiwa na kuisomwa aya ya sijda katika mkusanyiko mmoja mara mbili na tatu, basi inatosheleza sijda moja

Pili: Kurudia kisomo cha Aya za Sajadah tofauti Katika Matukio Tofauti.

Hali hii pia ni sawa kwa watu wanaosoma aya mbili tofauti za Sijda katika tukio moja. Kwa hiyo, ikiwa mtu atasoma aya moja ya sijda katika matukio mawili tofauti au akasoma aya mbili tofauti za sijda katika tukio moja, basi inatakikana kwa msomaji na msikilizaji kutekeleza au kurudia sijda ya kisomo mara tofauti kulingana na idadi ya mara zilizosomwa aya hizo zinazotofautiana.

Kwa hivyo, kwa mtu anayehifadhi aya na kurudia kisomo chake cha kukariri, inajumuishwa katika hali ya kwanza ambapo inatosha kwake kufanya sijda ya kisomo mara moja. Kwani mwenye kurudia kisomo kwa lengo la kuhifadhi anajumuishwa katika hali ya kwanza ambapo ni sunna kwake kusujudu mara moja tu.

Na anasema Mujaddid Ad Din Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhamamd Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: **'Mtu atakaesujudu kwa ajili ya Sujudu ya Kisomo cha Qur'an basi anatakiwa aombe Dua katika kusujudu kwake kulingana na maana ya yale yaliyozungumziwa ndani ya Aya husika, ya Sujud, ingawa na anaweza kufanya tasbih pia na Dua nyenginezo.'**

4-SIJDAT AS SAHW

❖❖❖❖

Sijdat As Sahw hua ni Sijda ambayo inajulikana kwa kiswahili kama Sijda ya Usahaulivu ambayo hutekelezwa kwa ajili ya kufidia kasoro zilizotokea ndani ya Sala ya Mtu husika, na hivyo kuainisha Umuhimu wa Kusimamia Ibada muhimu ya Sala Kiukamilifu.

Ambapo Sijdat As Sahw hua ni yenye kutekelezwa kutokana na Sababu kuu 3 zifuatazo:

1-*Az Ziyada* - Kuongeza Kitendo miongoni mwa vitendo vya Ndani ya Ibada ya Sala.

2-An Naqs -Kupunguza Kitendo miongoni mwa vitendo vya Ndani ya Ibada ya Sala.

3-*Ash Shak* - Kua na Shaka kuhusiana na kutekelezwa kwa Kitendo husika ndani ya Ibada ya Sala.

Ama tunapozungumzia kuhusiana na Az Ziyadah basi hua tunazungumzia kuzidisha kwa Idadi vitendo vya Ndani ya Ibada ya Sala kwa mfano, Kusimama, Kurukuu, Kukaa Kitako au Kusjudu.

Ambapo Mtu atakapozidisha idadi ya moja kati ya Vitendo hivyo kwa Makusudi ndani ya Sala basi Sala yake hio hua ni Batil.

Lakini Kama Mtu huyo anaesali atakua amefanya hivyo kuongeza kitendo cha ziada kutokana kusahau na kisha akawa hakuweza kukumbuka kuhusiana na usahaulivu huo hadi pale alipofikia mwisho wa Ibada ya Sala basi itambidi amalizie Sala hio kwa kufanya Sijdat Sahw na Sala yake itakua imetimia.

Na kwa upande mwengine basi Kama mtu huyo anaesali akakumbuka ndani ya Sala katika wakati wa Kuzidisha kitendo husika, basi itambidi aachane na kitendo hicho asiendelee nacho bali na aingie katika hatua nyengine ya Sala na kisha atakapomaliza Kusali kabla ya kutoa Salam basi itambidi kufanya Sijdat As Sahw.

Na hata kama Mtu akisahau kufanya *Sijdat As Sahw* kabla ya kutoa Salam basi kwa upande wa Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Yule anaesahau kusjudu kabla ya Kutoa Salam, basi hua ni mwenye kuweza kusjudu baada ya Salam na kisha atasoma Atahiyyat na kisha akatoa Salam tena.'**

Yaani kwa Mfano: Tusema Mtu anasali Sala ya Isha na kisha akajikuta amesali Rakaa 5 badala ya kusali rakaa 4 na kukumbuka kwake kua yuko katika Rakaa ya 5 wakati akiwa katika Attahiyat ya Mwisho, basi mtu huyo Humbidi kumalizia Attahiyat hio, kisha atasjudu Sijdat As Sahw mara mbili na kisha atatoa Salam.

Na kama ikiwa hakukumbuka kuhusiana na Rakaa hio ya 5 hadi baada ya kutoa Salam, basi Mtu huyo itambidi kufanya Sijdat Sahw baada ya Salam hio na kisha kutoa Salam tena.

Na kama itakua mtu husika atakumbuka baada ya Kuondoka alipokua akisali kua kumbe amesali Rakaa 5, basi hapa haitohitajika kwa mtu huyo kufanya Sijdat Sahw bali itahitajika kwake yeye kuirudia tena Sala hio yote tangu mwanzo hadi mwisho.

Kwani amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alitusalisha Rakaa Tano katika Sala ya Al Asr.**

Na baada ya Kumaliza Kusalisha, basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaulizwa na Masahaba *Radhi Allahu Anhum*: 'Ya Rasul Allah! Hivi Jee Imeshushuka Amri ya Ongezeko kwenye Sala?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akauliza: 'Kwanini?'**

Masahaba wakajibu kwa kusema: 'Kwa Sababu umetusalisha Rakaa Tano.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasjudu Sijda mbili baada yake.*(Sahih Muslim)*

Na amesema Ibrahim Ibn Aswad: **Alqaamah alitusalisha sisi Sala ya Al Asr kwa kusalisha Rakaa Tano**, **Ambapo baada ya Sala kumalizika basi Watu wakasema kumwambia Al Qaamah: 'Ewe Abu Shibl, Leo Umetusalisha Rakaa Tano.'**

Alqaamah akasema: La Sikufanya hivyo.

Watu wakasema: Kweli umetusalisha Rakaa Tano.

Ambapo Ibrahim Ibn Suwaid anaendelea kusema kua: 'Mimi nilikua pamoja na Watu hao waliosalishwa na nilikua ni Mtoto mdogo, lakini nikasema: Kweli Umetusalisha Rakaa Tano.

Alqamah akasema kuniambia mimi: 'Ewe Mwenye kuona kwa Jicho Moja, hata na wewe unasema hivyo hivyo pia?'

Ibrahim Ibn Suwaid anasema kua: Nami nikasema: 'Naam.'

Ambapo baada ya kupata Majibu hayo basi Alqamah akageukia Qibla na akasujudu mara mbili za Sijdat Sahw na kisha akatoa Salam.

Na Kisha Alqamah akasema: 'Amesema Abd Allah kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha sisi Sala ya Al Asr na kusalisha Rakaa Tano. Na alipomaliza na kugeuka basi Masahaba wakaanza kunon'gonezana baina yao miongoni mwao.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akauliza:Mbona Hivyo kuna nini?**

Masahaba wakauliza: 'Jee Ibada ya Sala Imeongezwa Kitu?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: 'La!'**

Masahaba wakasema: 'Ukweli ni kua Umetusalisha Rakaa Tano.'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akageukia upande wa Qibla na kisha akasjudu Mara mbili Sijdat Sahw na kisha akatoa Salam.Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Kwa Hakika mimi ni Mtu kama nyinyi, hua nnasahau kama mnavyosahau nyinyi.**

Ambapo Ibn Umayr anasema kua: 'Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hivyo pale inapotokea kua mmoja wenu akisahau ndani ya Sala basi ni Wajib asujudu Sijda mbili.'*(Sahih Muslim)*

Na Anasema Abd Allah Ibn Yusuf kua amesema Malik Ibn Anas kua amesema Ayoub Al Sakhtiyani kua:

عن أبي هُرَيرَة رَضِيَ اللهُ عَنْه، قال صلَّى بنا رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم إحْدَى صلاتَيِ العشيِّ – سمَّاها أبو هريرة، ولكن نسيتُ أنا– قال: فصلَّى بنا ركعتينِ، ثم سلَّمَ، فقام إلى :قال ابن سِيرين خشبةٍ معروضةٍ في المسجِدِ، فاتَّكأَ عليها كأنَّه غَضبانُ، ووضَعَ يَدَه اليُمنى على اليُسرى، وشبَّكَ بين أصابعِه، ووَضَع خَدَّه الأيمنَ على ظَهرِ كفِّه اليُسرى، وخرَجتِ السَّرَعانُ من أبوابِ المسجدِ، فقالوا: وعُمرُ، فهابَا أن يُكلِّماه، وفي القومِ رجلٌ في يديه طولٌ، يُقال قَصُرتِ الصَّلاةُ؟ وفي القومِ أبو بكرٍ له: ذو اليَدينِ، قال: يا رسولَ الله، أَنسيتَ أمْ قَصُرَتِ الصَّلاةُ؟ قال: لم أَنسَ ولم تَقصُر! فقال: أكَمَا يقولُ ذو اليدين؟ فقالوا: نعَمْ، فتقدَّم فصلَّى ما تَرَك، ثم سَلَّم، ثم كَبَّر وسجَدَ مِثلَ سُجودِه أو أطولَ، ثم رفَعَ رأسَه وكبَّر، ثم كبَّر وسَجَد مِثلَ سجودِه أو أطولَ، ثم رفَع رأسَه وكبَّر. فربَّما سألوه (أي: سألوا ابنَ سيرينثم سلَّم؟ فيقول: نُبِّئتُ أنَّ عِمران بن حُصَينٍ، قال: ثم سَلَّمَ

Amesema Muhammad Ibn Sirin kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha moja kati ya Sala za Jioni (Ambapo Imam Ibn Sirin anasema kua Abu Hurayrah Aliitaja Sala hio ila mimi nimeisahau) na akaihitimisha Sala hio baada ya Kuisalisha kwa Rakaa mbili tu. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka na kusimama kwenye karibu na Kigogo kilichopo mbele ya Msikiti na kuuweka mkono wake juu yake huku akiwa anaonekana kama kwamba amekasirika, akauweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto na kuvipitisha vidole vyake vya kulia baina ya vidole vyake vya kulia.

Ambapo Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* hawakuweza kusema chochote kutokana na kumuogopa na kumuheshimu *Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam*. Na wale Masahaba waliokua na Haraka wakaharakisha kutoka Nje, Huku wakiulizana kwa kusema: 'Vipi Leo Sala imefupishwa au?'

Hivyo Kuna Mtu aitwae Dhu Al Yadayn akamsogelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuuliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah Hivi Leo Sala Imefupishwa au umesahau?'

***Rasul Allah Sallallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La Haikufupishwa na wala Sikusahau.'**

Dhu Al Yadayn *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama haikufupishwa basi kwa hakika itakua Umesahau.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum:*'Hivi Jee Dhu Al Yadayn anasema kweli ama la?'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Naam, anasema Ukweli.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasimama. Na kusalisha Rakaa mbili zilizobakia ambazo alizisahau, na kisha akatoa Salam na akasema Allahu Akbar na kusjudu Sijdat ya Sahau ilizochukua mda wa kama Sijda za Kawaida au zaidi kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu

Akbar na kisha Akasema Allahu Akbar na Kusujud tena Sijda ya pili na kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar.'

Ambapo Imam Muhammad Ibn Sirin alipoulizwa kuhusiana na kua 'Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam kumalizia ama la?'

Basi Imam Muhammad Ibn Sirin akasema kua: 'Mimi nimeambiwa na Imran Ibn Husayn *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam'*(Bukhari na Muslim)*

Ambapo hii ni hadith inayotuonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisahau Rakaa mbili na kutoa Salam kabla ya kumalizika Sala.

Kwani kutoa Salam kabla ya kumalizia Ibada ya Sala husika hua ni kiongeza kitu ndani ya Sala husika,na atakaefanya hivyo kwa Makusudi basi Sala yake hua ni Batili.

Lakini kama akifanya hivyo kwa kusahau au kughafilika na kisha akakumbuka baada ya muda mfupi basi humbidi kumalizia Rakaa zilizobakia. Na kusjudu Sijdaat Sahw.

Lakini kama ikiwa amekumbuka baada ya mda kupita, basi mtu huyo humbidi kurudia tena upya kikamilifu Sala yake yote aliyoisali hapo kabla.

Na kwa mfano ikatokea kua Imam anasalisha Sala ya zaidi ya Rakaa mbili na kisha akatoa Salam baada ya Attahiyat ya kwanza kutokana na kusahau. Lakini baadhi ya Maamuma wakaja juu na kusimama na kuendelea na Rakaa zilizobakia kutokana na kujua kua bado kuna Rakaa za kumalizia.

Na Imam akakumbuka kua kumbe ilikua ni Rakaa ya pili na hivyo nae akaja juu katika kisimamo cha Rakaa zilizobakia na kuendelea kusalisha hadi mwisho, basi Imam itambidi atekeleze Sijdat Sahw.

Lakini kwa upande wa Maamuma ambao wao hawakutoa Salam basi watakua na hiari ya Kufanya Sijdat Sahw ama la katika Sala yao hio, lakini hata hivyo basi kama watamfuata na kutekeleza Sijdat Sahw pamoja nae basi itakua ni bora zaid kwao kwa sababu watakua ni wenye kumfuata Imam na kutoa Salam baada ya kutoa Salam Imam.

Ama kuhusiana na sababu ya pili inayopelekea kutakiwa kutekelezwa kwa Sijdat As Sahw ambayo ni An Naqs yaani kupinguza Kitu ndani ya Sala na hivyo inabidi tufahamishane vizuri kua kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua, Ibada ya Sala inajumuisha Sehemu kuu Tatu ambazo ni:

1-Nguzo za Sala Mambo ambayo ni ya Fardhi Katika Sala.

Na kutokana na kua kitendo husika kua ni Nguzo ya Sala basi kitendo hicho hua ni Fardhi au ni lazima kitekelezwe ndani ya Sala husika, kwani kisipotekelezwa basi Sala husika Hubatilika isipokua pale itakapotekelezwa Sijda As Sahw ndio Sala hio itakua inakubalika.

2-*Sunnah Ab'Adh* ambapo neno *BaAdh* linamaanisha Nusu, na hivyo sehemu hii hua inajumuisha Nusu ya Sunna Zote sa Sala ambazo hua ni Wajib kuzitekeleza.

Hivyo Mtu anaesali anatakiwa atekeleze Sunnah hizi kwa sababu ni Wajib na asipotekeleza kwa kusahau basi humbidi kutekeleza Sijda As Sahaw.

3-*Sunnah Hay'ah*ambapo neno Hay'ah hua ni lenye kumaanisha Kupamba, Kupendezesha, Kuongeza Thamani n.k ambapo hizi hua ni Nusu ya Sunna zilizobakia za Sala ambazo hukmu yake hua Si Fardhi wala si Wajib bali hua ni Sunnah na hivyo ukisahau basi hua haina haja ya kufanya Sijdat As Sahw.

Na katika kuyafafanua haya basi kwanza tunaanza na yale ambayo ni Fardhi ambayo ni Nguzo za Sala.

Ambapo tunapozungumzia Arkanu As Salat au Nguzo za Sala, basi hua tunazungumzia idadi ya vitu au mambo ambayo kinapokosekana kimoja tu miongoni mwake basi hupelekea Ibada Nzima ya Sala ya Mtu kua ni yenye kuporomoka.

Yaani kama vile inavyojengwa Nyumba ambayo ramani yake inatakiwa iwe na Nguzo nne kwa kila pembe kua na nguzo moja, lakini baada ya kupewa ramani basi fundi mwashi akajenga Nguzo tatu tu! Na hivyo kuidhoofisha pembe moja ya nyumba kwa kuikosesha nguzo.Na matokeo yake akaijenga Nyumba hio hadi ikamalizika,lakini baada ya kuhamiwa tu ikaporomoka na hivyo gharama zote na kazi yote ikawa bure, hivyo, hivyo pia ndivyo inavyokua Sala iliyopungukiwa Nguzo.

Na tunapozungumzia Nguzo za Sala basi hua tunazungumzia Mambo ambayo kwa upande wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi Wanazuoni wanasema kua kuna Nguzo 13 za Sala.

Na kwa upande wa Wanafiqh wa Madhhab mengineyo basi Wanasema kua Nguzo za Sala ni 14 na wengine wanasemakua ziko 17 na hii ni kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Hapa nataka tufahamiane kua ingawa Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Idadi yake kuanzia 13, 14 na 17.

Lakini ukweli ni kua hakuna tofauti ya Nguzo hizo baina ya Madhhab, kwani tofauti iliyokuwepo hua ni kutokana na namna ya kuzihesabu nguzo hizo.

Kwani kuna waliochanganya Nguzo mbili kwa pamoja wakahesabu kua ni Nguzo moja na kuna wanaosema kua la hizi ni nguzo mbili tofauti.

Hivyo hii tofauti ya Kiidadi isituchanganye na wala isitutie khofu wala wasiwasi au shaka kwani zote ni hizo hizo.

Labda nitoe mfano ili kuondoana shaka kwa kusema kua kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wamesema kua Kurukuu, Kunyanyuka, Kusjdu, na kukaa kitako baina ya Sijda mbili kua kila kimoja kati vitendo hivyo hua kinahesabika kua ni nguzo inayojitegemea ukijumuisha na Utulivu wa ndani ya kila kitendo.

Yaani kila kitendo hakiwezi kuhesabiwa hadi kiwe katika hali ya utulivu ndani yake na hivyo Utulivu wa ndani ya kila kitendo hua hauhesabiwi peke yake.

Lakini kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab mengine basi wao hua wanahesabu na Utulivu wa baina ya Sijda mbili kua ni Nguzo na kwao hua nguzo 14 na kuna wanaohesabu utulivu wa kila kitendo ndani ya nguzo hizi na hivyo kupata nguzo zaidi ya 14.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Amali ya mwanzo ambayo Mtu ataulizwa juu yake itakua ni Sala. Na ikionekana kua imekamilia basi Mtu huyo atakua Salama na mwenye Kufuzu**. **Lakini kama ikiwa haijakamilika basi Mtu huyo atakua ni Mwenye kukosa bahati na mwenye kula hasara.**

Hivyo kama zikionekana Kasoro zozote zile ndani ya Sala zake za Fardhi , basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataamrisha kua aangaliwe Mja wake kama anazo Sala zozote zile za Sunnah ili ajaliziwe juu ya Kasoro zilizokuwemo ndani ya Sala zake za Fardhi, na kisha Amali zake nyengine zitahesabiwa kwa mpangilio huo huo.'*(Imam At Tirmidhi)*

ARKANU SALAAT - NGUZO ZA SALA

❖❖❖❖

Neno Rukn kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha, Kuegemea, Nguzo, Kuamini, Kutegemea, Kusimamia Kitu ambacho ni Madhubuti, Kuunga Mkono, Sehemu Madhubuti ya Kitu, Mahkama, Majigambo ya Nguvuna Uwezo, Jeshi, Chama au Kikundi cha watu wenye Nguzu na uwezo wa Kutegemeana na Kutegemewa.

Kwani anasema *Allah Subahanh wa Ta'ala* katika aya ya Qur'an iliyotumia neno Rukn kua:

﴿فَتَوَلَّىٰ بِرُكْنِهِ وَقَالَ سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ﴾

Fatawall<u>a</u> biruknihi waq<u>a</u>la s<u>ah</u>irun aw majnoonun*(Surat Adh Dhariyyat 51:39)*

Tafsir: ***Lakini (Fir'awn) aliupa Mgongo (Uongofu wetu) pamoja na Watu wakena wakasema: 'Hakika huyu Nio Mchawi au ni Mwendawazimu'***

Na kisha *Allah Subahanh wa Ta'ala* akafafanua kulichofuatia baada ya hapo kwa kusema:

﴿فَأَخَذْنَاهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ فِي ٱلْيَمِّ وَهُوَ مُلِيمٌ﴾

Faakha<u>dh</u><u>n</u>ahu wajunoodahu fanaba<u>dh</u><u>n</u>ahum fee alyammi wahuwa muleemun*(Surat Adh Dhariyyat 51:40)*

Tafsir: ***Hivyo tukamkamata yeye na Jeshi lake na kuwatupa kwenye bahari huku akiwa yeye ndie mwenye Kulaumiwa.***

Na pia akasema katika aya ifuatayo kua:

﴿قَالَ لَوْ أَنَّ لِي بِكُمْ قُوَّةً أَوْ آوِيَ إِلَىٰ رُكْنٍ شَدِيدٍ﴾

Q<u>a</u>la law anna lee bikum quwwatan aw <u>a</u>wee il<u>a</u> ruknin shadeedin*(Surat Hud 11:80)*

Tafsir; ***Akasema Lau kama ningekua na nguvu dhidi yenu, au ningetegemea sehemu yenye Nguvu dhidi yenu.***

Ambapo wenye Lugha yao hua wanasema kua inaposemwa Rukn ya Mtu hua inamaanshwa Uwezo Wake Kinguvu na Ustahmilivu wake katika mambo mbali mbali, na inaposemwa kuhusiana na Rukn ya Mlima au Kitu chochote basi hua inamaanishwa Upande wake ulioegemea zaidi, na Rukn ya Jamii ya watu hua ni Kingozi wao mwenye ngvu na Uwezo zaidi yao.

Na kwa upande wa Imam Al Kafwi basi yeye anasema kua: '**Rukn ya kitu hua ni sehemu au kitu ambacho kitu husika hakiwezi kuwepo au kusimama kwake bila ya kuwepo kwa Rukn yake.**

Na hivyo hii ndio maana ya Rukn za Sala au Nguzo za Sala kwa sababu inapokosekana moja tu kati yao basi Sala husika hua haiwezikusimama na kuhesabika kua ni Sala.'

Ambapo kwa upande wa Imam Al Hajjawi basi yeye anasema kua: **'Rukn au Nguzo za Sala hua ni Kile kilichomo ndani yake ambacho kama hakiwezi kuachwa kwa makusudi, wala kwa kusahau wala kwa kutojua.'**

Na hivyo Nguzo hua ni tofauati na Sharti, kwa sababu Nguzo hua ni kile kinachowajibishwa kufanywa ambacho hua ni sehemu ya kitu husika, kwa mfano Nguzo za Sala hua ni Nia, Takbrat Al Ihram, Surat Al Fatiha, n.k.

Wakati Sharti hua ni kile kinachowajibishwa kufanywa lakini hua si sehemu ya kitu husika. Kwa mfano Masharti ya Sala ni kua Mtu lazima uwe na Udhu, Lazima uwe umeelekea Kibla, Iwe umeingia wakati wa Sala.nk

Ambapo Imam Shams Al Din Muhammad Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini anasema kua: **'Nguzo hua ni hali ambayo ni yenye ulazima wa kuhitajika na hutofautiana na Sharti kwa kutokana na kua Sharti hua ni kile kinachoitangulia Sala kabla ya kusaliwa ambacho hua ni lazima kitokee kabla kwa mfano kujitoharisha, kujihifadhi n.k na Nguzo hua ni kile kinachojumuishwa kufanyika ndani ya Sala kwa mfano Kurukuu, Kusujudu, n.k.'**

Na kwa upande wa Imam Wahba Al Zuhayli basi yeye anasema kua: **'Kilugha basi Sharti hua ni Alama, na Kishariah hua ni Kitu ambacho kuwepo kwake hua kunategemewa na kitu husikaambacho hua ni chenye kuwepo nje ya Kitu husika.'**

Ambapo Kilugha Nguzo hua ni Upande wenye Kutegemewa kinguvu,na Kisharia hua ni Kitu ambacho Kuwepo kwa Kitu husika hua kunategemewa kutokana nayo. Na hivyo hua ndio kitu cha ndani kabisa cha kitu husika.'

Kwa maana hio basi Nguzo na Masharti hua vinaelezewa kua ndio Misingi ya Sala na hivyo baadhi ya Wanazuoni wanasema kua ndio sehemu za Wajib za Sala. Ambapo kwa upane wa Masharti ya Sala basi hua kuna Masharti ya aina mbili ambayo ni Sharti la Wajibu na Sharti la Kukubalika.

Masharti ya Wajib hua ni Wajibu ambao Sala ya Mtu husika hua inategemeana nayo kwa mfano Mtu husika inabidi lazima awe Muislam, awe ni mwenye kutimiza umri wa kua ni mwenye Kubaleghe na awe ni mwenye kua na akili timam. Na Masharti ya Kukubalika kwa Sala hua ni yale yanayoifanya Sala husika kua ni yenye kukubalika kwa mfano, lazima kua na Udhu n.k

Na tunapozungumzia Vitendo vya Sala basi Wanazuoni wamevigawa kwa ujumla vitendo vya Sala katika hali Tatu Kuu ambazo ni Nguzo, Wajib na Sunnah, ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanahesabu Nguzo kua ni yale mambo ambayo hayatakikani kuachwa ndani yake iwe kwa makusudi au kwa kutokusudia kwani Sala hua ni yenye kubatilika yanapoachwa hivyo kama yakiachwa basi hubidi kuyarudia na kisha pia kuleta Sijdat Sahw badala yake., na Wajib ni yale mambo ambayo yakiachwa basi hua inabidi kuleta Sijdat Sahaw kwa ajili ya kufidia badala yake na Sunnah hua ni yale ambayo hua hayastahiki kurudiwa pale yanapoachwa iwe kwa makusudi au kwa kutokususida na wala haastahiki kulipiwa fidia ya Sijdat sahaw baada yake.

Ambapo Wanazuoni wametoufatisha mambo haya kutokana na maamrisho ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akiwafundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* namna ya kusali na pia alipokua akiwakosoa pale walipokua wakikosea kama tutakavyoona katika vitihibitisho vya hadith katika kurasa zinazfuatia.

Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Nguzo za Sala basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa Nuuman Ibn Thabit tunaona kua wao wanasema kua: **'Kuna Nguzo zaaina mbili, kuna Nguzo za Asili na kuna Nguzo za Ziada'**

‘Nguzo za Asili hua ni kile ambacho kinaweza kuachwa pale mtu husika anapokua hawezi kukitekeleza, na hivyo mtu husika hua hatakiwi kufanya kitu chengine badala yake. Na nguzo ya Zaidi hua ni kile ambacho hua kinaweza kuachwa kutokana na hali fulani mbali ya Mtu husika hua anaouwezo wa kutekeleza kitu hicho, kwa mfano Kusoma Surat Al Fatiha hua ni Nguzo ya Sala lakini pale Mtu anapokua Maamuma basi hua hatakiwi kuitekeleza kwa sababu ya kua mtu huyo ni mwenye kuongozwa ndaniya Sala yake na Imam ambae ni mwenye kuitekeleza Nguzo hio ya kisomo cha Surat Al Fatiha kutokana na kuisoma kwake ambako humtosheleza Maamuma wake.’

Kwa maana hio basi kukubalika kwa Sala hua kunategemeana na sehemu zake kuu ambazo ni nne yaani Kisimamo, Rukuu, Sujud na Visomo vilivyomo ndani yake, ambazo ndani yake mnajumuishwa Nguzo za Asili na Nguzo za Ziada, ambapo kikao cha mwisho cha Tahiyyat hua kinajumuishwa katika Nguzo ya ziada na baadhi yake nguzo hizo hua zimejumuishwa ndani yake.

Hivyo mtu atakapoacha moja kati ya nguzo hizinne basi hua ni mwenye kuhesabiwa kua si mwenye kusali na hivyo Sala yake hua haiwezi kuhesabiwa kua ni Sala. Ambapo mambo yanayojumuisha kukubalika kwa Sala hua yamegawika katika sehemu mbili ambazo ni:

Kwanza kile kilichomo nje ya Sala kabla ya kuanza kwa Sala ambacho ni Kujitiharisha kutokana na Uchafu na Najisi, Kujihifadhi sehemu za Siri, Kuelekea Kibla, Kuingia kwa wakati wa Sala husika, Nia na Ihram.

Pili kile kilichomo ndani ya Sala kivitendo kwa mfano Kusimama, Kurukuu, Kusujudu, ambavyo hua ndio msingi wa kuendela kuwepo kwa Sala, ama kuhusiana na Tahiyyat ya Mwisho basi basi hua ni Wajib na hii ni kutokana na Makubaliano ya Wanazuoni wao mbali ya kua wametofautiana juu yake kuhusiana na kama ni Nguzo ya Asili ama ni nguzo ya ziada.

Kwani kwa upande wa Allamah Abu Bakar Alaa Din Ibn Masud Al Kasani Al Samarqandi Al Hanafi basi yeye amesema kua: **‘Nguzo za Sala ni 6 ambazo ni Kisimamo, Kurukuu, Kusujud, Kisomo, ambapo Surat Al Fatiha hua ni Wajib, Kikao cha Tahiyyat ya Mwisho na mpangilio wa hatua za Sala.**’

Na anasema Imam Al Marginani Al Hanafi kuhusiana na Mtizamo wa Madhhabya Imam Abu Hanifa basi kuna:

1) *Shurūt* za Sala
1. Tohara ya mwili na Mavazi.
2. Tohara ya sehemu ya Kusalia.
3. Kujifunika Aura.
4. Kuingia kwa wakati wa Sala.
5. Kuelekea Kibla
6. Kua na Nia ya Sala Husika.

2) Nguzo au Faradhi za Sala:
1. *Takbira al Ihram*
2. *Qiyām* (Kisimamo).
3. *Qirā’ah* (Kisomo cha Qur’an).
4. *Rukū*ʿ.
5. *Sujūd*.
6. Tahiyyat ya Mwisho.

Wājibāt (Wajibu) wa Sala

1. Kusoma Sura h Al Fatihāh.
2. Kusoma Aya zisizopungua 3 baada yake.
3. Kusoma Surat Al Fatiha kabla ya aya 3 za ziada baada yake.
4. Kusoma Surat Fatiha na Aya 3 za Ziada katika Rakaa za mwanzo za Sala za Fardhi.
5. Kua na utulivu katika kila baada ya hatua ya Sala.
6. Kukaa Kitako katika Tahiyyat ya Mwanzo.
7. Kusoma Tahiyyat katika Vikao vyote viwili.
8. Kutoa Salam mwishoni mwa Sala.
9. Kusoma Qunut katika Salat ya Witr.
10. Kusma Takbira ya Idd.
11. Kusoma Kwa Sauti katika Sala za Sauti.
12. Kusoma kwa Sauti katika Sala za Kimya kimya.

2)Hakuna Dua baina ya Sijda mbili kulingana na mtizamo wa Imam Abu Hanifa, lakini hakuna tatizo kusema: **"*Allāhummagfirlī Warhamnī Wajburnī Wahdinī Warzuqnī*,"** kutokana na uthibitisho uliomo katika hadith iliyonukuliwa na Imam At Tirmidhi, Imam Ibn majah na Imam An Nasai.

3) Unaweza kusoma Dua yoyote iliyomo kwenye Qur'an na Hadith.*(Al hidaya Sharh Al Bidayah al Mubtadi - Imam A Marginani)*

Na tunapoangalia katika kitabu cha Fatawa Al Hindiyyah Cha Mkusanyiko wa Fatwa za Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi tuaona kua imesemwa kua:

Faraa'idh Salat ni:

1. Kusema Takbir ya kwanza.
2. Kusimama (Qiyam).
3. Usomaji wa Qur'an (Qira'ah).
4. Kufanya rukuu.
5. Kufanya sajdah.
6. Kukaa katika kikao cha mwisho kwa muda sawa na usomaji wa Tashahhud.

Wajibaat Salat ni:

1. Kusoma Sura h Al Fatiha katika rakaa mbili za mwanzo za Sala ya rakaa 3 na 4 na katika rakaa zote za witr na nafli.

2. Kusoma Sura h nyingine ambayo ima ni Aya tatu fupi, au Aya moja ndefu baada ya kusoma Al Fatiha katika rakaa mbili za mwanzo za Sala ya rakaa 3 na 4 na rakaa zote za witr na Nafli.

3. Kusoma Al Fatiha kwanza, na baada ya hapo Sura nyingine kwa mpangilio.

4. Kufanya kila tendo linalotokea zaidi ya mara moja moja baada ya jingine kwa mpangilio mfano kuingia kwenye Sijda ya pili mara tu baada ya Sijda ya kwanza.

5. Kufanya vitendo vyote vya Salah kwa wastani na utulivu.

6. Kusoma Tahiyyat katika kikao cha kwanza (baada ya kuinua kichwa kutoka kwenye sajda ya pili ya rakaa ya pili) na pia katika kikao cha mwisho.

7. Kusimama kwa rakaa ya tatu mara tu baada ya mtu kumaliza kusoma Tashahhud.

8. Kusali Dua ya Qunut katika Sala ya Witr.

9. Kutoa Takbir ya Sala ya Idi.

10. Ili Imam asome kwa sauti kubwa katika sala za Jum'ah, Eid, Tarawih, Witr ya Ramadhani, Alfajiri na katika rakaa mbili za mwanzo za Salah ya Maghrib na Isha. Mwenye kusali peke yake ana hiari ya kutaka kusali sala hizi kwa sauti au kimyakimya.

11. Kwa Imam na kwa ajili ya Salah moja peke yake (munfarid) kusoma kimya kimya katika rakaa mbili za mwisho za Isha salah, rakaa ya mwisho ya maghrib Salah, na katika Adhuhuri na Asr.

12. Kutoka kwenye Sala kwa salamu mbili.

Sunnah za Sala ni:

1. Kusimama moja kwa moja bila kusogeza kichwa wakati wa kusema takbira ya kwanza.

2. Kuinua mikono ya mtu sambamba na masikio ya mtu.

3. Kutazama viganja na vidole vya mikono ya mtu kuelekea kibla.

4. Wakati wa kunyanyua mikono kwa ajili ya takbira, kuacha vidole vyake jinsi vilivyo bila kuvitenganisha au kuviunganisha pamoja.

5. Kwa Mwanamme kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto chini ya kitovu; kwa kuweka kiganja cha mkono wake wa kulia juu ya sehemu ya nyuma ya mkono wake wa kushoto akikumbatia viganja vya mikono na kidole gumba na kidole kidogo.

6. Wanaume wanapaswa kutenganisha miguu yao kwa masafa ya vidole vinne baina ya miguu.

7. Kusoma Dua ya kufungulia Sala.

8. Kusoma Ta'awudh (A'uudhubillah) Dua ya kufungulia Sala.

9. Kusoma tasmiya mwanzoni mwa kila rakaa kabla ya kuanza Sura h Al Fatiha.

10. Kusema amiyn kimya kimya baada ya Al Fatiha.

11. Kusoma Sura h ndefu (Kuanzia Surat Al Hujuraat hadi Surat Al Buruj) katika Alfajiri na Adhuhuri, Sura h za urefu wa kati (Kuanzia Surat Al Buruj hadi Surat Al Bayyinah) katika Asr na Isha salah na Sura h fupi (Kuanzia Surat Al Bayyinah hadi Surat Al Naas) katika Salah ya Maghrib.

12. Kurefusha rakaa ya kwanza ya Fardh ya Alfajiri pekee.

13. Kusema 'Subhaanarabbiyal 'Adheem' mara tatu katika rukuu.

14. Kushika Magoti kwa mikono katika rukuu kutandaza vidole katika rukuu kwa Wanaume.

15. Kuweka miguu sawa katika rukuu.

16. Kwa Wanaume kuweka mgongo wao sawa katika rukuu, kuhakikisha kichwa kinasawazishwa na Kiuno.

17. Kwa Wanaume, upande wa ndani wa mikono yao kuwa mbali na mbavu zao

18. Kusoma 'Sami'allaahu limanhamidah' unapoinuka kutoka kwenye rukuu.

19. Kusimama kwa muda katika hali ya kusimama wima baada ya rukuu.

20. Kusoma 'Allahumma Rabbana walakalhamd' ukiwa umesimama wima kabla ya sajdah.

21. Wakati wa kufanya sajda, weka magoti kwanza, kisha mikono, na ndio kisha uso.

22. Kusema takbira wakati wa kwenda na kuinuka kutoka sajdah.

23. Kuweka kichwa katikati ya mikono katika sajdah.

24. Kusema ‘SubhaanarabbiyalA’laa mara tatu katika sajdah.

25. Kwa Wanaume, kuweka tumbo mbali na mapaja yake, visugudi mbali na mbavu, na mikono mbali na ardhi.

26. Visigino viwili kuwekwa pamoja katika sajdah.

27. Kwa Wanaume kutandaza mguu wa kushoto na kuinua mguu wa kulia, kuvifanya vidole vya miguu vielekee kibla. Mikono inapaswa kuwekwa kwenye mapaja.

28. Kunyanyua kidole cha shahada cha mkono wa kulia unaposema maneno ‘laailaaha’ ya tashahhud na kukishusha unaposema ‘illallaahu’.

29. Kusoma Salat Ibrahimiyyah baada ya Tashahhud katika kikao cha mwisho.

30. Kuifuata kwa kusoma du’a, kwa kutumia maneno yanayopatikana katika Qur’an au Hadithi. Du’a hiyo isiwe katika maneno ya watu wa kawaida.

31. Kutoa Salam kulia kwanza na baadae kushoto.

32. Wakati wa kutoa salaam, ili Imam hutoa kwa watu wote, Malaika na majini wema wanaomfuata. Kwa mwenye kusali nyuma yake, humtolea Imam, pamoja na watu, na kwa mwenye kusali peke yao huwatolea Malaika tu.

33. Salamu ya Imam na wanaosali nyuma yake iwe sawa.

34. Aliyechelewa kufika katika Salah amngoje Imam amalize salamu yake kwanza, kisha asimame ili amalizie salah iliyobakia.

Ama unaweza kusali dua nyingine kwa Kiarabu katika kikao cha mwisho (Qa’dahakheerah) au la, inajuzu kwa sharti kwamba dua hiyo iwe hivyo. Dua ambayo imetajwa katika Qur’an au Hadith. Mtu aombe dua kwa ajili yake mwenyewe, wazazi wake, na Waislamu wengine, hii ni sunna. Aseme dua iliyotajwa ndani ya Qur’an.

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ

“**Rabbanaa aatina fid dunya hasanatawwa fil aakhirati hasanataw waqina aadhaaban naar”.**

Ajiepushe na kufanya du’a inayofanana na maneno ya watu kama vile “Ewe Mwenyezi Mungu niozeshe hivi na hivi” hata kama inafanywa kwa Kiarabu, kwani kufanya hivyo kunaweza kuvuruga Sala.*(Al Fatawa Al Hindiyyah)*

Ama kuhusiana na Madhhab ya Imam Malik Ibn Anas basi wa wanasema kua Nguzo za Sala ni 15 ambazo ni:

1- Niyyah, ambayo hua haina haja ya kuitamka kwa maneno.

2-Takbirat Al Ihram huku ukiwa umesimama,

3-Kutamka Takbirat Al Ihram huku ukiwa umesimama,

4-Kisomo cha Surat Al Fatiha,

5-Kusoma Surat Al Fatiha huku ukiwa umesiamama,

6-Kurukuu,

7-Kusimama kutoka kwenye Rukuu,

8-Kusujudu,

9-Kukaa kitako baina ya Sijda mbili,

10-Tahiyyat ya mwisho,

11- Kukaa Kikao cha Tahiyyat ya Mwisho,

12-Kutoa Salam,

13- Kukaa huku ukiwa unatoa salam,

14-Kua na tulivu katika kila nguzo.

15-Kufuatisha utaratibu huu.

Sunnah za Sala kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik

Sunna za Sala zinajumuisha na vitendo ambavyo vinajulikana kama Mandub yaani vinavyopendekezwa, ambavyo ni 14:

1. Kusoma Aya nyengine baada ya Surat Al Fatiha katika Rakaa mbil za mwanzoni za Sala.
2. Kubakia katika kisimamao baada ya kusoma Surat Al Fatiha huku ukiwa unasoma Sura nyengine.
3. Kusoma kwa Sauti katika Sala za Sauti.
4. Kusoma Kimya Kimya katika Sala za Kimya Kimya.
5. Kutamka Takbirat Al Intikal katika kila hatua ya Sala.
6. Kusema Sami' Allahu liman hamidah" unaponyanyuka kutoka kwenye Rukuu, iwe peke yako au nyuma ya Imam.
7. Kusoma Tahiyyat.
8. Kukaa Kitako katika Tahiyyat.
9. Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Saam* katika Tahiyyat ya Mwisho"*Allahumma salli 'ala Muhammadin wa 'ala ali Muhammad kama sallayta 'ala Ibrahim wa 'ala ali Ibrahim wa barik 'ala Muhammadin wa 'ala ali Muhammadin kamâ barakta 'ala Ibrahim wa 'ala ali Ibrahim fi'l-'alamin innaka hamidun majeed*".
10. Kugusisha asehemu ya unyayo baina ya vidoa na mguu katika wakati wa Kusujudu, na kuweka Magoti na Mikono ardhi katika Sujud.
11. Kuitikia Salam ya Imam wako nay a Mtu wa Pembeni yako baada ya Kutoa Salam ya mwisho ya Sala.
12. Kutoa Salam kwa Sauti katika salam ya kutoka ndani ya Sala.
13. Kukaa kimya wakati Imam anapokua anasoma kwa sauti.
14. Kutimiza Wajibu wa Kutulia katika kila hatua.

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahamd Ibn Hanbal basi wao wanasema katika Dalil Al Taalib, ambao ni Mukhtasari maarufu unaotumiwa na Wanafiqh Wa Madhhab ya Imam Hanbali kua:

Nguzo za Sala ni 14 ambazo ni:

(1) Kusimama wakati wa sala ya faradhi ikiwa mtu anaweza kufanya hivyo.

(2) Takbira ya ufunguzi (kusema "Allahu akbar").

(3) Kusoma Al Faatihah.

(4) Rukoo' (kuinama), ambayo kidogo zaidi ina maana ya kuinama ili mikono iweze kugusa magoti, lakini umbo kamili zaidi unamaanisha kufanya usawa wa nyuma na kichwa sambamba nayo.

(5) Kuinuka kutoka kuinama.

(6) Kusimama wima.

(7) Sujud (kusujudu), ambayo umbo kamilifu zaidi ni kuweka paji la uso, pua, viganja vya mikono, magoti na vidole vya miguu kwa uthabiti juu ya ardhi, na ambayo kidogo zaidi ni kuweka sehemu ya kila moja ya hivi ardhini.

(8) Kuinuka kutoka kwenye sijda.

(9) Kukaa Kitako baina ya sijda mbili. Hata hivyo Kukaa Kitako mtu kunatosha, lakini Sunnah ni kukaa muftarishan, ambayo ina maana ya kukaa kwa mguu wa kushoto na kushikilia mguu wa kulia kwa kunyoosha vidole vya miguu vikielekea Qiblah.

(10) Kuwa na utulivu katika kila moja ya nguzo hizi za kimwili.

(11) Tashahhud ya mwisho.

(12) Kukaa kusoma tashahhud ya mwisho na salamu mbili.

(13) Salamu mbili. Hii ina maana ya kusema mara mbili, *"Al Salaamu 'alaykum wa Rahmat-Allah Wa Barakatuh)* Katika sala ya Sunnah inatosha kutoa salaam moja; hiyo pia inatumika kwa sala ya Jeneza.

(14) Kusimamia nguzo kwa mpangilio uliotajwa hapa. Iwapo mtu atasujudu kwa makusudi kabla ya rukuu, kwa mfano, Sala inabatilika; kama atafanya hivyo kimakosa, hana budi kurudi na kuinama, na kisha kusujudu.

Sehemu za faradhi za sala Upande wa Madhhab ya Imam Hanbal Ni 8 ambazo ni:

(1) Takbira zisizokuwa takbira ya ufunguzi

(2) Kusema "*Sami'a Allahu liman hamidah* (Mwenyezi Mungu Anawasikia wanaomhimidi" – kwa ajili ya Imam na kwa Maamuma.

(3) Kusema *"Rabbana wa laka'l-ham*d (Mola wetu Mlezi, sifa njema ni Zako)"

(4) Kusema *"Subhana rabbiy Al 'aziym (*Ametakasika Mola wangu Mlezi)" mara moja wakati wa rukuu.

(5) Kusema "*Subhana rabbiy Al a'laa* (Ametakasika Mola wangu Mlezi)" mara moja wakati wa kusujudu.

(6) Kusema "*Rabb ighfir li* (Mola nisamehe)" baina ya sijda mbili.

(7)Tashahhud ya kwanza.

(8) Kukaa Kitako kwa tashahhud ya kwanza.

Sunnah za maneno za maneno za Sala Upande wa Madhhab ya Imam Hanbal.

(1) Kusema baada ya takbira ya ufunguzi, ***"Subhaanaka Allahumma wa bi hamdika, wa tabaaraka ismuka, wa ta'aala jadduka wa laa ilaaha ghayruka*** (Utukufu na sifa ni Zako, ewe Mwenyezi Mungu, jina lako litukuzwe, litukuzwe utukufu wako. na hakuna mungu ila Wewe). Hii inaitwa du'aa' Al istiftaah (du'aa' ya ufunguzi)

(2) Kutafuta hifadhi kwa Mwenyezi Mungu.

(3) Kusema Bismillaah.

(4) Kusema Ameen.

(5) Kusoma soorah baada ya Al Faatihah.

(6) Kusoma kwa sauti, katika hali ya Imam.

(7) Kusema baada ya tahmiyd *(Rabbana wa laka'l-hamd)*, kwa asiyesali nyuma ya Imam: *"Mil' Al samawaati wa mil' Al ard wa mil' ma shi'ta min shay'in. ba'd* (Kuzijaza mbingu, na kuzijaza ardhi, na kuzijaza upendavyo). (Mtazamo sahihi ni kuwa pia ni Sunnah kwa mwenye kusali kwa jamaa)

(8) Kufanya tasbihi wakati wa rukuu zaidi ya mara moja, kama mara ya pili au ya tatu au Zaidi.

(9) Kufanya tasbihi katika sijda zaidi ya mara moja.

(10) Kusema "Rabb ighfir li (Mola nisamehe)" zaidi ya mara moja baina ya sijda mbili.

(11) Kusalia jamaa za Mtume *(Salla Allahu A'alayhi wa Aalihi wa Sallam)* katika tashahhud ya mwisho na kumletea baraka yeye na wao, na kuomba du'aa baada ya hayo.

Sunnah za matendo ya Sala kwa Upande wa Madhhab ya Imam Hanbal.

(1) Kuinua mikono wakati wa kufungua takbira.

(2) Kuinua mikono wakati wa kuinama.

(3) Kuinua mikono wakati wa kuinuka kutoka kuinama.

(4) Kuwaangusha baada ya hayo.

(5) Kuweka mkono wa kulia juu ya kushoto.

(6) Kutazama mahali pa kusujudu.

(7) Kusimama na miguu kando.

(8) Kushika magoti kwa vidole vilivyotawanyika wakati wa kurukuu, kunyoosha mgongo sawa na kukifanya kichwa kuwa sambamba nacho.

(9) Kuweka sehemu za mwili ambazo mtu anasujudia juu ya ardhi, mbali na magoti, kwa sababu ni makrooh kuzikandamiza kwa nguvu chini.

(10) Kuviweka visugudi mbali na ubavu, na tumbo na mapaja, na mapaja na mikono; kuweka magoti mbali; kushikilia miguu wima; kushikilia vidole kando juu ya ardhi; kuweka mikono kwa usawa na mabega na vidole kuviekeza Kibla.

(11) Kukaa mkao wa muftarishan baina ya sijda mbili na katika tashahhud ya kwanza, na kukaa mkao wa mutawarrikan katika Tashahhud ya pili.

(12) Kuweka mikono juu ya mapaja na vidole pamoja kati ya sijda mbili, na katika tashahhud, isipokuwa kwamba katika mwisho vidole vya pinkie na pete vishikwe ndani, duara lililofanywa kwa kidole cha kati na kidole gumba, na kimoja. inapaswa kuashiria kwa kidole cha shahada wakati wa kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala*

(13) Kugeuka kulia na kushoto wakati wa kutoa salaam

Kuna tofauti za maoni kati ya Wanazuoni kuhusiana na baadhi ya masuala haya; kinachochukuliwa kuwa ni faradhi na wengine kinachukuliwa kuwa ni Sunnah na wengine. Hili limejadiliwa kwa kina katika vitabu vya fiqh.

Na tunamalizia juu ya haya kwa kuangalia kuhusiana na Mtizamo wa Madhab ya Imam Abu Abdullah Muhammad Idris Al Shafii ambapo tunaona kua wao wanasema kua Sala ina nguzo 13, ambapoili Ibada ya Sala ikamilike basi lakini kuna mambo muhimu ya kuyatimiza ili Sala husika isiwe ni yenye kubatilika,ambayo ni:

Masharti (Shurut)

Masharti makuu ya Sala ni matano: (1) kuondoa uchafu (najasah), (2) tahara ya kiibada (tahara), (3) kuingia kwa wakati, (4) kufunika sehemu za siri(`awrah), na (5) kukabili uelekeo wa sala (qiblah).

Kuondoa Uchafu (Najasah)

1. Ifuatayo lazima isiwe na uchafu usio na udhuru: mwili wa mtu, kile ambacho mtu anaunga mkono, chochote hiki cha kugusa, na chochote kinachohusiana na kile ambacho mtu anaunga mkono.

2. Uchafu unajumuisha miili ifuatayo: (1) mbwa na nguruwe na kile kinachotoka kwao, (2) kinyesi kutoka sehemu za siri, (3) damu na usaha, (4) matapishi, (5) kilevi na (6) kila sehemu ya mnyama yeyote aliyekufa, isipokuwa maiti ya binadamu, nzige, viumbe vya majini, au wanyama wa kuliwa waliochinjwa. Sehemu yoyote iliyokatwa kutoka kwa mnyama hai ni kama mfu asiyechinjwa, isipokuwa nywele na mfano wa wanyama wanaoliwa.

3. Yote hayo hapo juu ni uchafu ndani yake yenyewe, na ikiwa mmoja wao atagusa kingo iliyo safi ndani yake, na unyevu kati yake, uchafu huhamishwa na hiyo ngumu hutiwa unajisi.

4. Uchafu ukigusa ujazo wa kimiminika, ujazo wote huani najisi, isipokuwa kama kiasi kikubwa cha maji, ambacho hua ni najisi pale uchafu huo utakapobadilisha sifa yake ya asili.

5.Yabisi iliyo najisi husafishwa kwa kuondoa athari za uchafu—mwili wake, ladha yake, rangi yake na harufu yake—na kisha kutiririka juu yake maji yasiyo najisi na ambayo hayajatumika, au ikiwa uchafu ni wa mbwa au nguruwe basi hutiririka maji yaliyopakwa matope juu yake mara moja na tambarare. maji juu yake mara sita.

Haya hapo juu yanahusu kujiondolea uchafu baada ya kutumia istinja , ingawa mtu anaweza kupangusa tu, badala ya kutumia maji, iwapo atatimiza masharti ya kupangusa.

6. Maji yanayotiririka juu ya sehemu iliyo najisi hutiwa unajisi yanapoguswa na najisi husika, isipokuwa pale inapokua dalili zote za Najis hio zilikuwa zimeisha ndani yake.

Usafi wa kiibada (Tahara)

1. Mtu lazima asiwe katika hali ya uchafu wa kiibada (hadathi), mdogo au mkubwa. Usafi mdogo wa kiibada huinuliwa kwa wudhuu (wudhu) na uchafu mkubwa wa kiibada huondolewa kwa kuoga (ghusl).

2. **Viungo vya udhu ni sita:** (1) Kutaka ruhusa kwa ajili ya Salah ya faradhi, wakati wa kwanza kuosha uso; (2) kuosha uso, mipaka yake ikiwa ni kutoka mahali ambapo mstari wa nywele ni kawaida hadi mwisho wa taya na kutoka sikio hadi sikio; kisha (3) kuosha mikono yote miwili kutoka kwenye ncha za vidole hadi kupita visugudi; kisha (4) kupaka majisehemu ya kichwa; kisha (5) kuosha miguu yote miwili mpaka vifundo vya miguu, ingawa mtu anaweza kuipangusa viatu badala ya kuosha miguu, ikiwa atatimiza masharti ya kupangusa; na (6) utaratibu uliotajwa.

3. Mambo manne yanabatilisha wudhuu: (1) chochote kinachotoka katika sehemu za siri; (2) kugusa moja kwa moja sehemu za siri za mtu yeyote au mkundu kwa sehemu ya ndani ya mkono; (3) kugusana ngozi kwa ngozi na mwanamke aliebalegh, anayeweza kuolewa nawe; na (4) kupoteza ufahamu.

4. Wenye ulazima wa kukoga ni watano ambao ni wenye: (1) Kumwaga manii, (2) Kujamiiana, (3) Hedhi, (4) kitanda cha mtoto (nifas), na (5) Kuzaa.

5.Viungo vya kuoga ni viwili: (1) Kutaka ruhusa kwa ajili ya Salah ya faradhi, wakati wa kuanza kuosha mwili, na (2) kuosha mwili mzima.

6. Ni muhimu kwa kutawadha na kukoga maji yasiyo najisi na yasiyotumika yanapita juu ya kila kitu kinachopaswa kuoshwa.

Ni lazima pia mtu ajue kuwa udhuu na kuoga na mambo yake muhimu yaliyotajwa katika maandishi haya ni wajibu.

Kuingia kwa Wakati

1. Ni lazima mtu aamini kwamba wakati wa Sala umeanza, kwa kubainisha kwa uhakika au ujasiri kupitia makadirio, lakini si kwa kufuata tu makadirio ya mtu mwingine anapoweza kujikadiria mwenyewe.

2. Wakati wa Sala ya alfajiri huanzia alfajiri, na Salah ya Adhuhuri linapopita jua kwenye kilele chake, na Sala ya Alasiri inapopindukia kivuli cha kitu chochote na urefu wa kivuli chake wakati wa adhuhuri. , ya Sala ya kuchwa kwa jua (Maghrib) wakati wa kuzama kwa jua, na ya sala ya Isha inapotoweka jioni nyekundu.

Kufunika sehemu za Siri (Awrah)

Mtu lazima avae kizuizi kinachoficha ngozi ya sehemu za Siri kutoka pande zote isipokuwa chini. Sehemu za aibu za Mwanamme ziko kati ya kitovu na magoti na za Mwanamke zote isipokuwa uso na mikono. Mtu lazima ahakikishe kufunika sehemu nzima kwa kufunika kidogo zaidi yake.

Kukabili Muelekeo wa Sala (Qiblah)

Ni lazima mtu akabiliane na mwelekeo halisi wa maombi, kwa kuuamua kwa uhakika, uhakika wa karibu, au ujasiri kupitia makadirio, lakini si kwa kufuata tu makadirio ya mtu mwingine anapoweza kujikadiria mwenyewe.

Masharti Mengine

Mtu lazima pia ajue kwamba Sala tano za kila siku na mambo muhimu yaliyotajwa katika hapa hua ni wajibu.

Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanakubaliana kua kuna aina nne za Nguzo ndani yake ambazo ni: **Rukn Qawli (Nguzo za Kauli), Rukn Fiil (Nguzo za Vitendo), Rukn Qalbi (Nguzo ya Moyo ambayo ni Nia) na RuknTartib (Nguzo ya kufuatisha mpangilio au utaratibu wa kila hatua ya Sala), ambapo zote kwa pamoja zinajumuishwa na kugaiwa katika hali ya kua Nguzo 5**

Tano kati yao ni *Rukn Qawliyyah* yaani nguzo za Kauli na Nguzo 8 Saba ni *Rukn Fiiliyyah* yaani Nguzo za Vitendo na Nguzo moja ni ya Moyoni.

Yaani kama ilivyosemwa katika Safinat Salat kua:

القَوْلِيَّة، وَهِيَ خَمْسَةٌ: تَكْبِيرَةُ الإِحْرَام أَوَّلُ الصَّلَاة، وَقراءة الفاتحةِ فِي كُلِّ رَكْعَةٍ وَقِرَاءَةُ التَشَهُّد وَالصَّلَاةُ عَلَى النَّبِي والسَّلامً آخِر الصَّلاة، ثلاثتها فِي القَعدةِ الأَخِيرَةِ

Qauliyyah ni Tano ambazo ni: Takbirat Al Ihram Mwanzoni mwa Kuingia dani ya Sala, Kusoma Surat Al Fatiha katika Kila Rakaa. Kusoma Tahiyyat ya Mwisho, Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat Ya Mwisho na Kutoa Salam ya kwanza ya kutokea Nje ya Sala.

Na Nguzo nane ni za kivitendo, ambazo ni: **Nia, kusimama katika jambo la Fardhi kwa wale wanaoweza, rukuu, kuinuka kutoka humo, sijda ya kwanza na ya pili, kukaa baina yao, kikao cha mwisho, na kufuatisha utaratibu huo. Ama utulivu ni sharti la rukuu, kusimama wima, kusujudu, na kukaa, na ni muhimu; hata ikiwa si nguzo ya ziada kwa mujibu wa rai iliyo sahihi zaidi.**

Hivyo Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii Nguzo 13 za Sala Kimpangilio ni:

1-Niyyah.

2-Takbirat Al Ihram.

3-Qiyyam.

4-Qiraat Surat Al Fatiha.

5-Ruquu.

6-I'tidal - Kusimama kutoka katika Rukuu na kusimama moja kwa moja.

7-Sujud.

8-Kukaa kitako baada ya kutoka katika Sijda.

9-Kutulia baina ya Sijda mbili.

10-Tashahud.

11-Kukaa kitako katika Tashahud ya mwisho

12-Taslim.

13-Tartib.

Na kwa kua walengwa wa Kitabu ni Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafi basi hatutofafanua zote hapa jambo ambalo hua ni kwa kifupi kama tulivyofanya juuya Mitizamo ya Mdahhab mengine, bali tutafanua kwa kuangalia Nguzo moja baada ya moja kwa kina, na hiyvo tunaanza na Nguzo ya kwanza ambayo ni Nia.

1-AN NIYYAH

Niyyah maana yake kilugha hua ni kusudio au lengo au madhumuni. Na hivyo kiibada hua inamaanisha kutaja madhumuni ya kitendo ukifanyacho au unachotaka kukifanya katika wakati wa ufanywaji wa kitendo hicho.

Ambapo kwa kila Ibada katika Dini ya Kiislam hua ni yenye kutakiwa kufanywa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala tu*. Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُواْ ٱلزَّكَوٰةَۚ وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلۡقَيِّمَةِ﴾

Wama omiroo illa liyaAAbudoo Allaha mukhliseena lahu alddeena hunafaa wayuqeemoo alssalata wayu/too alzzakata wadhalika deenu alqayyimati.*(Surat Al Bayyina 98:05)*

Tafsir: ***Na hawakuamrishwa (Watu) isipokua Kumuabudu Allah pekee kwa Ikhlasi bila ya kumshirikisha, na kujitolea katika Dini kiukamilifu kusimamisha Sala na kutoa Zakkah na hio ndio Dini iliyonyooka kimsimamo.***

Hivyo Nia hua ni yenye kukisafisha kitendo cha Ibada kutokana na kua si chenye kufanywa kwa ajili ya mwengine yeyote yule isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuusafisha Moyo kutokana na kua na kitu chochote kile ndani yake katika Ibada husika isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* Mola wa Viumbe wote, Mola ambae si mwenye kuhitaji chochote kutoka kwa Viumbe wake, kwani yeye peke yake ndie Mwenye uwezo wa juu ya kila kitu na ni mwenye kujitosheleza, na viumbe wake ni dhaifu kwake na wasiokua na uwezo wowote wa kumnufaisha, kumuathiri wala kumpunguzia kitu juu yake bali ni wenye kuhitaji kila kiu kutoka kwake na ni wenye kuneemeshwa kila kitu kutokana na Rehma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Hivyo ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee ndie anaestahiki kuabudiwa, na hivyo ukifanya vyenginevyo basi hua ni mwenyekubatilisha Ibada yako, na kuingia kwenye kumshirikisha*Allah Subhanah wa Ta'ala* .Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿ أَلَا لِلَّهِ ٱلدِّينُ ٱلۡخَالِصُۚ وَٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُواْ مِن دُونِهِۦٓ أَوۡلِيَآءَ مَا نَعۡبُدُهُمۡ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَآ إِلَى ٱللَّهِ زُلۡفَىٰٓ إِنَّ ٱللَّهَ يَحۡكُمُ بَيۡنَهُمۡ فِي مَا هُمۡ فِيهِ يَخۡتَلِفُونَۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَهۡدِي مَنۡ هُوَ كَٰذِبٞ كَفَّارٞ﴾

Ala lillahi alddeenu alkhalisu waalladheena ittakhadhoo min doonihi awliyaa ma naAAbuduhum illa liyuqarriboona ila Allahi zulfa inna Allaha yahkumu baynahum fee ma hum feehi yakhtalifoona inna Allaha la yahdee man huwa kadhibun kaffarun.*(Surat Az Zumar 39:3)*

*Tafsir:****Kwa hakika ikhlasi katika Dini ni kwa ajili ya Allah pekee. Ama kwa wale ambao ni wenye kuwachukua Miungu wengine zaid yake Allah Subhanah wa Ta'ala huku wakisema kua Tunwaabudu wao ili wapate kutukaribisha karibu na Allah Subhanah wa Ta'ala , basi Allah Subhanah wa Ta'ala atahukumu baina yao wote juu yay ale waliyotofautiana juu yake. Kwa hakika Allah hawaongozi wale wenyekudumu kwenye Uongo na Kufru.***

Hivyo tunaweza kusema pia kua **Nia hua ni Maamuzi ya Ndani ya Moyo wa Mja katika Kufanya Ibada kwa ajili ya kujikaribisha Kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee.**

Kwani Nia katika Ibada ndio kitu kinachotofautisha baina ya kitendo kinachofanywa kua ni Ibada si Ibada bali ni mazoea tu. Kwa maana hio basi Kitendo cha Ibada hua si chenye kuhesabika kisharia kua ni Ibada kama ikiwa hakina Nia ndani yake, na hivyo mfanyaji wa kitendo husika kisichokua na Nia ndani yake hua hakina malipo ya Ibada mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* .

أَخْبَرَنَا عَمْرُو بْنُ مَنْصُورٍ، قَالَ حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ مَسْلَمَةَ، قَالَ حَدَّثَنَا مَالِكٌ، وَالْحَارِثُ بْنُ مِسْكِينٍ، قِرَاءَةً عَلَيْهِ وَأَنَا أَسْمَعُ، عَنِ ابْنِ الْقَاسِمِ، قَالَ أَخْبَرَنِي مَالِكٌ، عَنْ يَحْيَى بْنِ سَعِيدٍ، عَنْ مُحَمَّدِ بْنِ إِبْرَاهِيمَ، عَنْ عَلْقَمَةَ بْنِ وَقَّاصٍ، عَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ، رضى الله عنه – وَفِي حَدِيثِ الْحَارِثِ أَنَّهُ سَمِعَ عُمَرَ يَقُولُ – قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " إِنَّمَا الأَعْمَالُ بِالنِّيَّةِ وَإِنَّمَا لِامْرِئٍ مَا نَوَى فَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ فَهِجْرَتُهُ إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ لِدُنْيَا يُصِيبُهَا أَوِ امْرَأَةٍ يَتَزَوَّجُهَا فَهِجْرَتُهُ إِلَى مَا هَاجَرَ إِلَيْهِ "

Kwani Umar Ibn Mansur kua amesema Abd Allahi Ibn Maslamah kaua amesema Malik na Harith Ibn Miskin kua nimemsikia Ibn Qasim kua amesema Malik kua amesema Yahya Ibn Said kua amesema Muhammad Ibn Ibrahim kua amesema Alqaamah Ibn Waqqas kua amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua;'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Vitendo hua ni kulingana na Nia, na kila mtu atalipwa kulingana na Nia yake, yeyote yule aliefanya Hijra kwa ajili *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi Wa Salam* basi atalipwa Hijra yake kwa ajili *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi Wa Salam* na aliehama kwa ajili ya mambo ya Kidunia au kwa ajili ya Kuoa Mwanamke, basi atalipwa Hijra yake kwa ajili ya kile alichokifanyia Hijra.*' *(Bukhari na Muslim)*

Ambapo amesema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua '**Hadith hii ni Nusu ya Ilm ya Dini ya Kiislam kuhusiana na Ilm ya Dini ya Kiroho na kimwili,kwani amali hua ni muonekano wa nje wa vitendo ambavyo muonekano wa ndani yake hua ni Nia. Na Hadith hii inajumuisha mas-ala 70 ya Ilm ya Fiqh.'**

Hivyo nia ni Moyoni na ni udhihirishwaji wake hua ni wa hali inayotamkwa. Na tunapoiangalia Ibada ya Sala basi tunaona kua inajumuisha sehemu nnezitokazo ndani ya mwili wa Ibn Adam ambazo ni Kauli (Qawl), Vitendo (Fi'il), Akili Kiroho (Ma'nawi)na Moyo (Qalbi), ambapo Nia ndio kitu pekee kitokacho katika sehemu ya Qalbi yaani Moyoni utekelezwaji wake ni kabla ya *Takbirat ul Ihram*, na Mtu atakaesoma Takbirat Al Ihram bila ya Nia basi Sala yake hua ni Batili.

Ambapo anasema Imam Sulaiman Ibn Muhammad Ibn Umar Al Bujaraimi kwenye*Hashiyyah Al Bujaraimi ala Sharh Minahj Al Tulab* kua: **'Kwa ujumla, kiwango cha nia katika sala imegawanywa katika Ngazi nne, ambazo ni:**

Ngazi ya kwanza : Istihdar Haqiqi (استحدار الحقيقة); hiyo ni kuwasilisha nia juu ya nguzo nzima ya maombi kwa undani.

Ngazi ya pili: Muqaranah Haqiqiyyah (مقارنة الحقيقية); yaani ni pamoja na Nia mwanzoni mwa usemi wa takbira mpaka mwisho wa usemi.

Ngazi ya tatu: Istihdar 'Urfi (استحدار العرفي) ; yaani kuwasilisha Nia juu ya nguzo za sala kwa ujumla tu.

Ngazi ya nne: Muqaranah 'Urfiyyah (مقارنة العرفية); yaani kujumuisha Nia katika sehemu ya takbira ima mwanzoni, katikati au mwisho wa takbira.'

Na kwa upande wa Imam Abu Zakarriyah Sharaf Al Nawawi basi amesema kua: **'Nia lazima iambatane na Takbira, na ikasemwa: Mwanzo unatosha Maana yake : "Ni wajibu kujumuisha nia pamoja na Takbir. Kwa kuzingatia mtazamo dhaifu: inatosha (nia) mwanzoni mwa Takbir".**

Kimsingi, Imam Al Khatib Al Shirbini amesema kua;'**Nia ya sala lazima ijumuishwe wakati wa kutamka Takbiratul Ihram kwa sababu Takbir ni nguzo ya kwanza katika Salah . Nia pia lazima iingizwe mwanzoni mwa Takbir na iendelee hadi mwisho wa Takbir (muqaranah Al haqiyyah).'**

Hata hivyo, kwa kuzingatia mtazamo usio wa mwisho wa Madhhab ya Imam Al Shafi'i, inatosha kwa mwenye kusali kuwasilisha nia mwanzoni mwa takbira na si wajibu kujumuisha nia mpaka mwisho.

Kwani Imam Abu Maali Al Haramain al Juwaini na Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhamamd Ibn Muhamamd Ibn Muhammad Al Ghazali basi wao waliona kwamba jambo hili lilikua gumu kwa Ummah kulitekeleza. Kwa hiyo, wanaona kuwa si wajibu kujumuisha nia mwanzoni mwa takbiratul ihram na kudumu mpaka mwisho. Inatosha hata kwa Ummah kujumuisha nia ya Salah kwa namna ya muqaranah urfiyyah na huu pia ni mtazamo uliochaguliwa na Imam Al Nawawi na mtazamo wenye nguvu katika Madhhab ya Imam Al Shafii.

Wanachuoni hawakubaliani wanapofafanua maana ya muqaranah urfiyyah. Kwani Imam Al Shafii Al Saghir Shams Ad Din Al Ramli anaeleza kuwa ni kuhusianana kua kama mtu ajumuishe nia katika Salah ima mwanzoni, katikati au mwisho wa takbira. Wakati huo huo, baadhi ya wengine wanaifafanua kuwa nia wakati wa kusema takbir katika hali ambayo yeye hapuuzi kuikumbuka na kufuata kwa uzito kamili .

Imam Al Bujairimi pia alisema kwamba kuna maoni kutoka kwa baadhi ya Wanazuuoni wa karibuni kutoka katika Madhhab ya Imam Al Shafi'i ambayo yanapunguza nia katika suala la istihdhar urfi na muqaranah urfiyyah kwa sababu ngazi mbili hizi za mwanzo hazina uwezo wa kufanywa na watu wa kawaida.

Ambapo kwa upande mwengine wa kukosekana kwa nia mwanzoni mwa Takbir, yaani ikiwa nia haikutamkwa mwanzoni mwa Takbir, basi ImamAl Bujayrimi anasema Juu ya hili kua**: 'Imam Al Subki amesema kua: Wanazuoni wetu wamekhitalifiana kuhusiana na pendekezo hili, ikasemekana kwamba kinachokusudiwa ni kuendelea kutamkwa, lakini kutamka nia sio nia, na si kuthibitisha yasiyokuwa nia, hakuna dalili juu yake.'**

Na Mfuatano wao Nia na Takbir Al Ihramhua ni zinazofanana kwani ikipatikana nia inayozingatiwa Ndani ya Moyo kwanza, basi hupatikana kitu mithili yake, na pia ikiwa haukupatikana muda wa kutofautisha baina yao, na kutamka nia si sawa na kutamkaTakbir at Ihramambako huleta madhara isipotamkwa, kwa sababu sala haiwezi kutimia inapokosekana Takbirat al Ihram.

Hivyo Niyyah nikua na Nia ya kujua kwa Moyo wakati wa Sala Husika, na kujua kua Sala hio inasaliwa kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Na kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hua ni Sunna kuitamka Nia hio ya Sala husika kwa kauli mara tu unapotaka kuisali Sala hio kabla Takbirat Al Ihram.

Ambapo ndani yake nia hio basi Mtu anatakiwa aseme anataka kusali Sala gani Yaani kama ni Fardhi ama ni Sunna, na kisha alitaje Jina la Sala husika kama Fajr, Dhuhr, au Kablia au Baadia n.kyaani kama katika hali zifuatazo.:

أُصَلِّيْ [سُنَّةَ/فَرْضَ] الصلة[الصُّبْحِ/الظُّهرِ/الجمع /العَصْرِ/المغْرِبِ/العِشاَءِ] [الْقَبْلِيَّةَ/الْبَعْدِيَّةَ]
[رَكَعَتَيْنِ/ثَلاَثَرَكَعاَتٍ/اَرْبَعَرَكَعاَتٍ] اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ [اِمامً/مَأْمُوماً] لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallee [Sunnata/Fardha] Salati [As-Subhi/Ad-Dhuhri/Jumuah/Al Asri/Al Maghribi/Al 'Ishaa'i] [Al Qabliyyatan/Al Ba'diyyatan] [Raka'ahtayni/Thalaatha Raka'aatin/Arba'a Raka'aatin] adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati [Imaaman/Ma'muuman] lillahi Allahu akbar.

Nanuia Kusali Unataja aina ya Sala(Sunna ama Fardhi) Jina la Sala(Subhi, Dhuhr, Jumaah, Al Asr, Maghrib Isha) Idadi ya Rakaa(Rakaa 2,3,4) nikiwa nimeelekea Qibla Kama Imam au Maamuma kwa ajili ya Allah, Allahu Akbar.

Hivyo Nia ya Sala husika katika Sala za kila siku hua kama ifuatavyo:

أُصَلِّيْ سُنَّةَ الصلة الصُّبْحِ رَكَعَتَيْنِ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Sunnat Salat as-subhi rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi Allahu Akbar.

Maana yake**: "Ninakusudia kusali rakaa 2 sunna za Subhi nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar."**

Nia ya Fajr Fardh.

أُصَلِّيْ فَرْضَ الصلةالصُّبْحِ رَكَعَتَيْنِ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Fardh Salat as-subhi rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi Allahu Akbar.

Maana yake**: "Ninakusudia kusali rakaa 2 Fardh ya Subh nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar."**

Nia ya Rak'ah 2 Dhuhr Kabla ya Sunnat

أُصَلِّيْ سُنَّةَ الصلة الظُّهرِ الْقَبْلِيَّةَ رَكَعَتَيْنِاَدَاءًمُّسْتَقْبِلاًاِليالكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Sunnat Salat ad-Dhuhr i-l qabliyyatan rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi Allahu Akbar.

Maana yake: **"Ninakusudia kusali rakaa 2 kabla ya Sunnat ya Dhuhr nikielekea kibla kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"***

Nia ya Dhuhr Fardh

أُصَلِّيْ فَرْضَ الصلةالظُّهرِ اَرْبَعَ رَكَعاَتٍ اَدَاءًمُّسْتَقْبِلاًاِليالكَعْبَةِالشَّرِيفَةِ لِلهِاَللهُاَكْبَرْ

Usallii Fardh Salat ad-Dhuhr i arba'a rak'aahtin adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi Allahu Akbar.

Maana yake: **"Ninakusudia kusali rakaa 4 Fard ya Dhuhr nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Nia ya Salat Jumaa Fardh.

أُصَلِّيْ فَرْضَ الصلة الجمع رَكَعاَتِين اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلِي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Fardh SalatAl Jumaah rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi Allahu Akbar.

Maana yake: **"Ninakusudia kusali rakaa 2 Fardh ya Ijumaa nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Nia ya Rak'ah 2 Baada ya Dhuhr Sunnat

أُصَلِّيْ سُنَّةَ الصلة الظُّهرِ الْبَعْدِيَّةً رَكَعَتَيْنِاَدَاءًمُّسْتَقْبِلاًاِليالكَعْبَةِالشَّرِيفَةِ لِلهِاَللهُاَكْبَرْ

Usallii Sunnat Salat ad-Dhuhr i-l ba'diyyatan rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi Allahu Akbar.

Maana yake: **"Ninakusudia kusali rakaa 2 baada ya Sunnat ya Dhuhr nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar."**

Nia ya Rakaa 2 za Kabla ya Asr Sunnat.

أُصَلِّيْ سُنَّةَ الصلة العَصْرِ رَكَعَتَيْنِ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلِي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Sunnat SalatAl 'asri rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake: **"Ninakusudia kusali rakaa 2 sunna za 'Alasiri nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar**

Nia ya 'Asr Fardh

أُصَلِّيْ فَرْضَ الصلةالعَصْرِ اَرْبَعَ رَكَعاَتٍ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلِي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Fardh SalatAl 'asri arba'a rak'aahtin adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake**: "Ninakusudia kusali rakaa 4 Fard ya 'Asr nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Nia ya Maghrib Fardh

أُصَلِّيْ فَرْضَ الصلةالمغْرِبِ ثَلاَثَ رَكَعاَتٍ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلِي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Fardh SalatAl maghribi salaasa rak'aahtin adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake: "**Ninakusudia kusali rakaa 3 Fard ya Maghrib nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Nia ya Rak'ah 2 Maghrib Baada ya Sunnat.

أُصَلِّيْ سُنَّةَ الصلة المغْرِبِ الْبَعْدِيَّةً رَكَعَتَيْنِ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلِي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Sunnat SalatAl maghribi-l ba'diyyatan rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake**: "Ninakusudia kusali rakaa 2 baada ya Sunnat ya Maghrib nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Makusudio ya Rak'ah 2 'Ishaa Kabla ya Sunnat

أُصَلِّيْ سُنَّةَ الصلة العِشاَءِ الْقَبْلِيَّةً رَكَعَتَيْنِ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلِي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Sunnat SalatAl 'ishhaa-il qabliyyatan rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi Allahu Akbar.

Maana yake**: "Ninakusudia kusali rakaa 2 kabla ya Sunnat ya Ishaa nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Makusudio ya 'Ishaa Fardh

أُصَلِّيْ فَرْضَ الصلةالعِشاَءِ اَرْبَعَ رَكَعاَتٍ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلِي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Fardh SalatAl 'ishaa-i arba'a rak'aahtin adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake: **"Ninakusudia kusali rakaa 4 Fard ya 'Ishaa nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Makusudio ya Rak'ah 2 Baada ya 'Ishaa Sunnat

أُصَلِّيْ سُنَّةَ الصلة العِشاَءِ الْبَعْدِيَّةَ رَكَعَتَيْنِ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallii Sunnat SalatAl 'ishaa-il ba'diyyatan rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake: **"Ninakusudia kusali rakaa 2 baada ya Sunnat ya 'Ishaa nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala Allahu Akbar"**

Nia ya Rak'ah 2 Witr

أُصَلِّيْ صَلٰوةَ الْوِتْرِ رَكَعَتَيْنِ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallee Salah at Al witri rak'atayni adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake**: "Ninakusudia kusali rakaa 2 Witr Salah nikielekea kibla kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala *Allahu Akbar"***

Nia ya 1 Rak'ah Witr

أُصَلِّيْ صَلٰوةَ الْوِتْرِ رَكَعَتٍ اَدَاءً مُّسْتَقْبِلاً اِلي الكَعْبَةِ الشَّرِيفَةِ لِلهِ اَللهُ اَكْبَرْ

Usallee Salah at Al witri rak'ahtin adaa-am mustaqbilan ilal k'abati-s sharifati lillahi allahu akbar

Maana yake**: "Nakusudia kusali rakaa 1 Witr Salah nikielekea kibla tukufu kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala *Allahu Akbar***

Naam..kama Sala husika haitokua Sala ya Fardhi basi itatosheleza Kutia nia kwa kutaja jina la Sala bila kusema kama ni Sunnah au Fardhi .

Lakini kama ni Sala ya Fardhi basi haitotosheleza kutaja Jina la Sala bila kusema maneno Fardha Salati, kwani kwa Sala ya Fardhi basi maneno haya lazima uyataje.

Na tunapozungumzia Nia ya Sala basi hua tunazungumzia Kitu ambacho kinaenda Sambamba na Takbir ya mwanzo, yaani ni lazima kua na nia ya Sala husika ndani ya Akili na Ufahamu wako wakati unasema Takbir ya Kwanza yaani Allahu Akbar.

Hivyo haitakiwi kufanya chochote au kufikiria chochote ambacho kitapelekea kukukosesha Umakini katika Nia yako.

Na kama Sala ikiwa ni Sala ya Jamaa inayojumuisha Wanaume na Wanawake basi Imam wa Sala hio anatakiwa abainishe hilo kwa kusema katika nia yake kua: ***Ana Imamn Liman TabiA'ani***yaani Mimi Ndie Imam kwa wale wanaonifuata.

Hivyo Imam anatakiwa abainishe katika Nia kua yeye ndie Imam wa Sala husika kama vile ambavyo inavyotakiwa kwa Maamuma kubainisha katika Nia kua yeye ni Maamuma wa Sala husika.

KUBADILISHA NIA YA SALA NDANI YA SALA.

❖❖❖❖

Ama kwa upande mwengine basi hua kuna hali mbili ambazo zinazoweza kujitokeza kwa Mtu anaesali peke yake huku akiwa na ni ya kua anasali peke yake Sala husika.

Lakini katika Kusali kwake basi mara akaja Mtu akaanza kusali nyuma yake na kuanza kumfuata, basi huyu anaefuatwa hua anaruhusika kubadilisha nia yake ndani ya Moyo wake kua sasa hivi mimi ni Imam wa wanaonifuata.

Ambapo hali ya pili basi labda kwa mfano mimi nimefika Msikitini kwa ajili ya kusali Sala ya Adhuhuri na Jamaa imeshamalizika, na kisha nikatia nia kusali pembeni peke yangu.

Lakini katika Wakati nnasali nikiwa katika Rakaa ya kwanza basi wakaja watu wakajipanga na Imam wao kwa ajili ya Kusali Sala ya Adhuhuri pia nami nikajikuta nimo kwenye Safu yao kutokana na wingi wao

Basi inapotokea hali kama hii hua pia inaruhusika kubadilisha nia ndani ya Sala kutoka katika hali ya Kusali peke yangu na kuingia katika hali ya Maamuma ili kunufaika na Jamaa.

Ila sasa kwa sharti la kua lazima uwe katika Rakaa sawia Na Imam, au Yeye Kakutangulia yaani wewe usiwe uko mbele Kirakaa kuliko Imam.

Hivyo nia inaweza ikabadilika kutoka katika hali ya mtu anaekua anasali peke yake na kua Imam au Maamuma. Kama tulivyosema hapo awali ambapo kama alivyofafanua Imam Al Khatib Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shibrini katika *Al Mughni Al Muhtaj*.

Na amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Kuna siku mimi nililala kwenye Nyumba ya Shangazi yangu *Ummu Ul Muuminina* Maymunah Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliamka akasali sala ya Qiyam Al Layl Ambapo na mimi nikaamka na kujumuika nae na kusimama kwenye upande wake wa kushoto Lakini mara *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanivuta mimi kwa kichwa changu katika upande wa kulia kwak**e.'*(Sahih Bukhari)*

عَنْ جَابِرٍ، قَالَ صَلَّى مُعَاذُ بْنُ جَبَلٍ لأَصْحَابِهِ الْعِشَاءَ فَطَوَّلَ عَلَيْهِمْ فَانْصَرَفَ رَجُلٌ مِنَّا فَأُخْبِرَ مُعَاذٌ عَنْهُ فَقَالَ إِنَّهُ مُنَافِقٌ . فَلَمَّا بَلَغَ ذَلِكَ الرَّجُلَ دَخَلَ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَأَخْبَرَهُ بِمَا قَالَ مُعَاذٌ فَقَالَ لَهُ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " أَتُرِيدُ أَنْ تَكُونَ فَتَّانًا يَا مُعَاذُ إِذَا أَمَمْتَ النَّاسَ فَاقْرَأْ بِالشَّمْسِ وَضُحَاهَا وَ {سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الأَعْلَى}

Na amesema Jabr Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua:**Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* alikua akisali pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Na kisha alikua akitoka na kuenda kuwasalisha watu wake. Siku Moja alisalisha Sala ya Isha na ndani yake akasoma Surat Al Baqara. Ambapo mmoja kati ya Maamuma akaacha Kusali Sala hio, na Muadh alipojua kuhusiana na Mtu huyo basi akawa ni mwenye kumlaumu.**

Habari hizi zikamfikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alimwita na kumwambia Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* kua: Ewe Muadh, unawatia watu kwenye Mitihani, Unawatia Watu kwenye Mitihani, Unawatia Watu kwenye Mitihani Hivyo unaposalisha basi soma Surat kama Washams, Sabihisma Rabbika Al Aala n.k *(Bukhari na Muslim)*

Na kutokana na hadith hii basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakariyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii ya Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Muadh *Radhi Allahu Anhu* kua:

'Hadith hii inathibitisha kua inaruhusika kwa yule Mtu anaesali Sala ya Fardhi kusali Nyuma ya yule anaesali Sala ya Sunnah. Kwa Sababu Muadh *Radhi Allahu Anhu* alikua akisali Sala ya Fardhi na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na hivyo kua tayari ni mwenye kutekeleza Wajibu wake wa Sala ya Fardhi.

Na kisha Alikua akienda kwa Watu wake na Kusali mara ya pili pamoja nao, kwa maana hio Sala yake hio ilikua ni Sunnah kwake yeye lakini hapo hapo ilikua ni Fardhi kwa Watu wake.

Hili ni Jambo ambalo limezunguzmiwa tena katika Sahih Muslim na hii inakubalika kulingana na Mtizamo wa Imam Al Shafii *Radhi Allahu Anhu* na wengineo.'(*Sharh Sahih Muslim)*

Na amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali katika mwezi wa Ramadhan Na mara mimi nikajiunga na kusali nyuma yake kulia kwake,na mara akaja mtu mwengine akajiunga pia na akaja mwengine na kujiunga hadi ikawa ni kundi zima Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipojua kua niko nyuma yake basi akaifanya Sala yake hio kua ni fupi***.** *'(Sahih Muslim)*

Ambapo kwa mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Abu Hanifa basi ni kua: **'Haikubaliki kwa Imam na Maamuma kua na Nia Tofauti katika Sala moja yaani kama Imam anasali Sunna basi haikubaliki kwa Maamuma kumfuata kwa ajili ya Sala ya Fardhi kama tulivyooona kwenye ifano ya Hadith tulizoziangalia, bali kama Imam anasali Sala ya Adhuhuri basi na Maamuma inabidi awe na nia ya Sala ya Adhuhuri, n.k na hii ni kwa kutokana na uthibitisho wa Hadith isemayo kua: 'Imam amechaguliwa kwa ajili ya kufuatwa' na kwa maana hio basi Maamuma humbidikumfuata hadi kwenye Nia'**

Ambapo wa wale wasemao kua Inakubalika kumfuata Imam hata kama ni mwenye kua na nia tofauti na Maamuma kwa sababu Hadith ya Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* inafahamisha kua: **'Sala ya Imam na Maamuma hua ni kulingana na Vitendo vya muonekano wa nje wa Mtu anaesali, kama ilivyokua kwenye Hadith ya Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* hivyo Jamaa hua si lazima kujumuisha Nia moja ndani yake'.**

Ambapo anasema Imam Ibrahim Ibn Muhamamd Ibn Ahmad Al Bajuri Al Shafii kua: **'Hua haiathiri kitu tofauti baina ya Nia ya Imam na Maamuma, na hivyo hua inakubalika kwa Mtu anaesali Sala ya Fardhi kua Maamuma wa Mtu anaesali Sala ya Sunnah na Mtu anaesali Sala ya Fardhi kua Maamuma wa anaesali Sala ya Qadha, na watu wanaosali Sala ndefu wanaweza kua Maimam wa Wanaosali Sala fupi kama Adh Dhuhr au Subh n.k'***(Hashiyyah Al Bajuri)*

Hivyo inafaa kwa mwenye kusaliSala ya Fardhikusali nyuma ya mwenye kusaliSala nyingine ya Fardhi, mfano Imam anayesaliSala ya Adhuhuri nyuma ya Imam anayesaliSala ya Alasiri.Haya ni mafundisho ya Imam Al Shafii, na Hadithiliyotoka kwa Ahmad, nayo ni itikadi ya Madhahiri.Hivi ndivyo walivyosema kundi la Salaf, na likakubaliwa na Imam Ibn Al Mundhir, Imam Al Saanani, Shyakh Ibn Taymiyyah, Shaykh Ibn Baz, na Shaykh Ibn Uthaymin pia.

Na inapojuzu kusaliSala ya Fardhi nyuma ya mwenye kusaliSala ya hiyari, hii inaashiria kuruhusiwa kwa nia ya anayesaliwa nyuma kuwa tofauti na ile ya Imam. Na vithibitisho vya Hadith havikuweka sharti la kua lazima kuwe na Nia ya Sala ya aina Moja baina ya Imam na Maamuma; Hii inaashiria kuwa ikiwa nia ya Imam na mwenye kusali nyuma yake itakhitalifiana, kama mmoja wao akikusudia kusali na mwengine kusaliSala ya Sunna au mmoja anakusudia kusaliSala ya Alasiri na mwengine anakusudia kusali Sala ya Adhuhuri, kisha Sala ya jamaa ni halali.

Kwa sababu hakuna chochote kilichothibitishwa kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hilo linaashiria ulazima wa kuunganisha makusudio ya Imam na mtu anayesaliwa nyuma. Na

Kinachoamrishwa ni kumfuata Imam katika yale yanayoonekana kuwa ni matendo yake, lakini nia haipo kwetu, na chochote kisichokuwa kwetu sisi hatulazimiki kufanya hivyo.

Na Sala ya Fardhi nyuma ya Sala ya Sunna Sala ya Fardhi iliyo nyuma ya Sala ya Fardhi hua ni sahihi, kulingana na mtizamo wa Madhehebu ya Imam Al Shafii, na iliypia kwa Mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal, na Imam Ibn Al Mundhir, Imam Al Saananiy na Shaykh Ibn Taymiyyah, Imam Al Shawkani, Shaykh Ibn Baz, na Shaykh Ibn Uthaymiyn pia.

Na hili tunaliona pia katika Hadith ya Jabir, *Radhi Allahu Anhu* amesema: **'Tulikwenda pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mpaka tukakaa mahali pamoja na akataja Hadithi. kuhusu Sala ya khofu... mpaka akasema: Kisha ukaitishwa wito wa kusali, basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasali rakaa mbili kwa kundi moja, kisha wakachelewesha." Na nyingine, kundi lilisali rakaa mbili, kwa hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikuwa na rakaa nne, na rakaa mbili kwa watu.**'

Na Kutoka kwa Abu Bakra*Radhi Allahu Anhu* amesema: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali kwa khofu adhuhuri, na baadhi yao walijipanga nyuma yake na baadhi ya miongoni mwao. wakawakabili maadui, akasali pamoja nao rakaa mbili, kisha akatoa salamu, kisha wakaondoka wale waliosali naye wakasimama katika misimamo ya Masahaba zao, wakaja wakasali nyuma yake, akasali nao rakaa mbili.', kisha ikasema salamu, ambayo ilikuwa rakaa nne kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na rakaa mbili kwa Masahaba zake.'**

Ambapo katika Hadith hii tunaona kua*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokuwa akisalisha rakaa mbili kwa kila kundi, alikuwa katika moja ya Sala mbili hizo anasali Sala ya Sunna, na Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua wakimfuata.

Na pia anasema Amr Ibn Salamah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Sisi tulikua tukiishi na Baba yetu katika njia ya Misafara inayoelekea Madina Munawwarah. Hivyo wakati Misafara ilipokua ikipita kutokea Madina basi ilikua ikipita Kijijini mwetu, nasi tulikua tuiwauliza Wasafiri kuhusiana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo nao walikua wakituambia kua alikua akidai kua anapokea Ujumbe kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na walikua wakitusomea baadhi ya Aya za Qur'an kututhibitishia kuhusiana na Madai yake.**

Nami nilikua nikizihifadhi Aya hizo, na kupitia katika njia hii basi nilikua nikijua vizuri sana kuhusiana na Qur'an kabla ya hata kuingia katka Dini ya Kiislam. Makabila yote ya Mabedui yalikua yakisubiri Mji wa Makkah Mukarramah kujisalimisha chini ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Na katika *Fat-hu Makkiya* (Ufunguzi wa Mji wa Makkah) watu wote kutoka katika Makabila ya Kibedui yakajisalimisha kwa *Rasul AllahSalallahuu Alayhi wa Salam* na kuingia katika Uislam.

Na Baba yangu alikua ndie Kiongozi wa Watu wetu aliekwenda kwa *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kufunga makubaliano ya Kuungana nae kwa niaba ya Kabila letu. Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akawafundisha kuhusiana na Sala na mambo mengine ya msingi katika Uislam. Na kisha akawaambia: 'Unapowadia mda wa kusali basi mmoja wenu Ataadhini na kisha Mtu mwenye kuijua zaidi Qur'an Miongoni mwenu ndio anatakiwa awe Imam wenu katika Sala.'

Watu wangu wakamtafuta mwenye Ilm zaidi ya Qur'an katika kabila langu lakini wakashindwa kumpata zaidi yangu, hivyo kwa kua hakukua na Mtu mwengine mwenye kujiua zaidi Qur'an katika kabila langu zaidi yangu basi mimi nikachaguliwa kua ndio Imam katika wakati huo, huku nikiwa na umri wa miaka sita au saba. Na niliwaongoza watu katika Sala na pia katika Mazishi yalipokua yakitokea.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo hii ni hadith inayotuonesha mambo kadhaa ndani yake ikiwemo kukubalika kwa Mkubwa kua in mwenye kusali nyuma ya Mdogo kulingana na Ilm yake mtu husika. Na kua inatakiwa kumfuata

Imam katika yale matendo yanayoonekana dhahiri bila ya kujali umri wake, kwani muhimu ni kua awe na sifa stahiki za kua Imam.

Ama kuhusiana na Kusali Sala ya Sunna nyuma ya Imam anaesalisha Sala ya Fardhi ni sahihi, na hili linaafikiana na Madhehebu manne ya Fiqhi: Madhhab ya Imam Hanafi, Madhhab ya Imam Maliki, Madhhab ya Imam Shafii na Madhhab ya Imam Hanbali, nayo ni itikadi ya Madhhab ya Zahiri, na kuna Ijmaajuu ya hilo.

Na hii ni kutokana na hadith ya Abu Said Al Khudhri *Radhiya Allaahu 'Anhu* ambae anasema kua**: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuona mtu mmoja akisali peke yake na akasema: 'Je, hakuna mtu anayeweza kutoa sadaka kwa hili? , ili aweze kusali pamoja naye'***(Imam Abu Daud)***

Maana ya Hadith hii ni kua Sala ya Jamaa hua ni kwa kundi lililosali Sala yao ya Fardhi, kwa hiyo Sala yao hii hua Sala ni ya Sunna baada ya Sala ya Fardhi.

Kwani Amesema Abu Dharr*Radhi Allahu Anhu*kua'***Anhu***: ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **aliniambia: 'Utafanyaje ikiwa una watawala juu yako wanaochelewesha Sala kuliko wakati wake? Nikasema: Unaniamrisha nifanye nini? Akasema: Sali Salah kwa wakati wake, na ukiipata jamaa ya pamoja na watu, basi Sali pia, kwani hua ni Sala ya Sunna kwako.'**

Na amesema Yazid Ibn Al Aswad Al Amiri ***Radhi Allahu 'Anhu*** **kua**: **'Nilishuhudia pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisali Sala ya alfajiri katika Msikiti wa Al Khaif, alipomaliza kusali akakuta watu wawili nyuma ya Jamaa ambao hawakusali pamoja naye, akasema: Nini kilichokuzuieni kusali pamoja nasi? Watu hao Wakasema: Ya Rasul Allah, hakika sisi tumesali tukiwa safarini.Akasema: Basi msifanye hivyo. Kwani Mkisali Mkiwa safarini, basi mkifika kwenye Msikiti wenye Jamaa basi Salini nao; Kwani Sala hio ni hua ni Sala ya Sunna kwenu.**

Hivyo Kinachoamrishwa ni kumfuata Imam katika yale yanayoonekana kuwa ni matendo yake, lakini si katika Nia kwani Nia hua haiko dhahiri na hua inamhususu mhusika peke yake. Tofauti baina ya nia ya Imam na mwenye kusali nyuma yake katika Sala haidhuru, na hii ni kwa sababuSala hua ni Ibada moja, hata kama wakati utakua unatofautiana, Kwa sababu kanuni za Sala hazibadiliki kulingana na nia na Kilichoamrishwa ni kumfuata Imam katika yale yanayoonekana kuwa ni matendo yake, lakini kuhusu nia yake hua haipo kwetu, na chochote kisichokuwa nasi sisi hatuhusiki nacho.

Na ingawa hua inakubalika Kubadilisha Nia ndani ya Sala kama tulivyoona hapo kabla kwa mtu mwenye kusali peke yake kua Imam,au Maamuma kua anaesali pekee yake lakini pia kwa upande mwengine basi, moja ya mambo yaliyobatilisha Salah ni kitendo cha kubadili nia ya Salah yenyewe husika kuingia katika Sala nyengine. Kama asemavyo Imam Al Khatib Al Sharbini amesema:

'Jambo la sita linalobatilisha Salah ni kubadili nia na kuwa jambo ambalo halikusudiwa mwanzo; basi ikiwa mtu atabadilisha Salah anayosali kwenye Salah nyingine kwa makusudi, basi Salah yake inabatilika.'*(Al Mughni)*

Ambapo Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawiy anasema katika Al Majmuu kua: **'Kama mtu ataingia ndani ya Sala ya Fardhi na kisha akabadilisha Nia yake kuingi kwenye Sala nyengine ya Fardhi au ya Sunna, basi hua ni mwenye kujibatilishia Sala yake hio aliyomo ndani yake na hua si mwenye kupata chochote kutokana na kila alichokinuia, na hii ni kama ilivyoelzewa na Imam Ahmad na Imam Abu Hanifa.**

Hivyo kakam mtu akinuia kuingia kwenye Salat Adh Dhuhr nakisha akabadilisha nia na kua ni mwenye kuingia Salat Al Asr, basi Sala yake ya Al Asr hubatilika kwa sababu sio Sala aliyoinuia, na Sala yake ya Adhuhuri hua ni batili na hii ni kwa sababu hakuinuia katika wakati alipoingia kwenye Sala hio. Na kama kaibadilisha nia Salat Al Asr yake kuifanya kua ni Sala ya Sunna, basi Sala yake ya Al Asr hubatilika kutokana na kama tulivyosema hapo kabla.'

Ambapo hua kuna mtiizamo miwili kuhusiana na Sala ya Sunnah, kwani kuna mtizamo wa kua hua haisihi kutokana na kile tulichokisema kuhusiana na Salat Al Asr. Na kuna mtizamo usemao kua Sala hio ni sahih kwa sababu Nia ya Sala ya Fardhi hua ni yenye kujumuisha Sala ya Sunnah ndani yake, na hii ni kutokana na ushahidi wa ukweli wa kua yeyote yule atakeaingia katika Salat Adh Dhuhr kabla ya wakati wa Sala ya Adh Dhuhr na kudhania kua ni baada ya Adh Dhuhr basi Sala yake hio aliyoisali hua ni Sala ya Sunnah.*(***Al Majmuu)***

NIYYAH YA SALA ZA FARDHI NA SUNNAH NA MASHARTI YAKE.

❖❖❖

Kwa kua Salahua ama ni Fardhi ya mtu binafsi, kama ilivyo sala tano za kila siku; au ni Fardhi ya jumuia, kama Sala ya Jeneza au Maiti na Sala ya Nadhiri, au ni Sunna iliyothibitishwa au isiyothibitishwa,n.k

Ama kuhusiana na Nia ya Salah za Fardhi, basi maelezo yake kulingana na Madhhab ni kama ifuatavyo:

Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wanasema kua: Kuna mambo yanayohusiana na mada hii: Moja wapo ni kwamba ni wajibu kwa kila Mtu mwenye kua na Umri wa Kubalegh kujua kuwa *Allah Subahanah wa Ta'ala* amemuwajibishia Sala tano.

Na hivyo kama ikiwa mtuhajui kuhusiana na Sala za Fardhi, basi Salah yake haiwi sawa hata ikiwa atasali kwa nyakati zake, isipokuwa atasali pamoja na Imam na akakusudia Sala ya Imam wake. Ikiwa anajua kuwa ana Sala ya Fardhi, lakini hatofautishi baina ya Sala ya Fardhi na Sala ya Sunna na hivyo akazisali zote kwa nia ya Fardhi, basi Sala yake ni sahihi;

Hili ni jambo la kawaida miongoni mwa watu wa kawaida, ijapokuwa Sala yao kwa namna hii, ijapokuwa ni sahihi, ni lazima wajifunze kutofautisha baina ya Fardhi na sala nyingine, na wasiendelee na ujinga wao wa kutojua mambo ya lazima ya dini yao bali wawe ni wenye kutafuta I'lm ili wapate kujua wasiyoyajua.

Pili: Namna ya kutia nia, na jinsi ya kuweka nia katika Salah ya Fardhi: ni kwamba mwenye kuabudu anaijua moyoni mwake Sala anayosali, sawa ikiwa ni Dhuhr, Asr, Maghrib, Isha, au Alfajiri. Anapojua hilo, basi ameweka nia, ambayo ni sharti la lazima kwa ajili ya usahihi wa sala. Basi ikiwa umeingia wakati wa Salah, basi inatosha kubainisha wakati wa Sala husika bila ya kuongeza chochote, hivyo ikiwa atakusudia kusali Sala ya Dhuhr, Alasiri, au Sala nyingine za Fardhi, basi Salah yake ni sahihi, kwa hivyo hawi. kutakiwa kukusudia Dhuhr ya leo au Dhuhr ya wakati huo; na baadhi yao husema: Bali anatakikana kukusudia Dhuhr ya leo au Dhuhr ya wakati huo, kwa sababu wakati wa kusali unakubali Sala nyingine ya Fardhi kuwa ni Sala ya Qadha, hivyo ikiwa anakusudia Salah ya Dhuhr, inawezekana akawa anamaanisha. Dhuhr leo, na inawezekana kwamba anamaanisha Salah ya Dhuhr wakati huo, basi hana budi kuifanya, na rai zote mbili ni sahihi, ingawa ni tahadhari zaidi kukusudia Dhuhr leo au Asr. leo. Hii ni ikiwa sala iko kwa wakati.

Hata hivyoikiwa ni nje ya wakati, na alikuwa hajui mwisho wa sala, basi Inatosha kwake kukusudia kusali Dhuhr au Alasiri bila kizuizi juu ya uwezekano mkubwa, na ikiwa anajua kuwa wakati umepita, inasemwa kuwa inatosha, na inasemwa kuwa haitoshi, na kwa hali yoyote. ni hadhari zaidi kuiwekea mipaka siku, hivyo anasema: Dhuhr leo, au Alasiri leo, na akikusudia kusaliSala ya Fardhi bila ya kubainisha, haimtoshelezi isipokuwa atakapobainisha katika Nia yake pamoja na wakati, na hiyo ni kwa kukusudia kusaliSala ya Fardhi ya wakati huo, hivyo ikiwa ana nia ya kusaliSala ya Fardhi ya wakati huo, basi inajuzu kwa sharti kwamba Sala hiyo iwe ndani ya wakati; kwa hivyo ikiwa atasali baada ya muda kupita, na hajui kuwa imepita na akakusudia Sala ya Fardhi ya wakati huo, basi hii hua si sahihi.

Kwa maana hio basi hua kuna ulazima wa katika Nia kwa Mtu anaetaka kusali kubainisha muda anaokusudia kusali, hivyo ikiwa atasali kwa wakati wake, basi bainisho la Nia hua ni kwa nia ya Salah yenyewe ya Fardhi, iwe Dhuhr au Alasiri n.k.; na baadhi yao wanaamini kwamba kubainisha haitoshi ndani yake, bali ni lazima anuie kwa kusema Asr ya leo au Magharibi ya leo, n.k; na ikiwa atasali baada ya muda kupita na hajui kuwa wakati wa Sala husika umepita, basi mfano wake ni sawa na mwenye kusali kwa wakati wake, inatosha kwake kukusudia Dhuhr au Alasiri bila ya kuongeza chochote zaidi, kinachowezekana zaidi; Ikiwa alijua anajua kwamba wakati umepita, basi atatumika Nia hio hio. Baadhi yao wanasema inatosha kwake kukusudia kusali Dhuhr au Alasiri n.k., bila ya nyongeza yoyote. Baadhi yao wanaamini kwamba ni lazima kukusudia ya Dhuhr leo.

Hivyo, kama ikiwa Mtu hakubainisha aina ya Sala kwa mfano kama Dhuhr au Asr, n.k na hakuiwekea ndani ya mipaka siku hiyo. Bali alikusudia tu sala ya Fardhi . Basi hii hua haitoshelezi na hii ni kutokana kwa makubaliano ya Wanazuoni. Ikiwa alikusudia Sala ya Fardhi ya wakati huo, basi nia yake hua ni sahihi kama ikiwa Sala yake hio ilikuwa katika wakati wake.

Tatu: Nia katika Sala ya Jeneza na sala ya Fardhi ambayo hua ni sharti la kuhalalika kwake. Kama ilivyo sharti la kuhalalisha Sala ya Fardhi, na kama Sala ya Jeneza, inatosha kwake kukusudia Salah ndani yake, lakini makusudio kamili ndani yake ni kukusudia Sala ya Jeneza na kuumuombea Mtu husika aliyekufa, na kama anakusudia Salah ya Ijumaa ndani yake, basi kama vile nia ni sharti la kuhalalisha Salah ya Fardhi kwa mujibu wa Mahanafi, pia ni sharti la kuhalalisha Salah ya Fardhi, mfano Witr na rakaa mbili za Tawaf, kwani nia ni sharti la uhalali wao, kwa kukusudia Witr na Rakaa mbili za Tawaf;

Vile vile inatumika kwa sala ya Sunna ambayo alianzisha na kisha kuharibu. Iwapo alianza kusali rakaa mbili kwa hiari yake kisha ikaharibika Salah yake kabla ya kuimaliza, ni lazima airudie. Katika hali hii, nia inahitajika, kwa sababu kuwaomba mara ya pili imekuwa wajibu. Kwa ufupi ni kwamba nia inatakiwa kwa ajili ya Sala za Fardhi, iwe ya mtu mmoja peke yake au ya pamoja kwa Jamaa, na ya Fardhi na ya nadhiri. Ama katika Sala ya Sunna, Nia hua haihitajiki.

Madhhab ya Imam Maliki basi wanasema kua: Makusudio ya Fardhi ni lazima ibainishwe, kwa kukusudia katika Nia kua ni Sala ya Adhuhuri au Alasiri, n.k. na hivyo kama ikiwa Mtu hakukusudia Sala husika kua ni Sala maalum ya Fardhi , basi Sala yake hua si sahihi.

Madhhab ya Imam Al Shafii basi wanasema kua: Kuna Masharti yafuatayo kwa Nia yaSalah ya Fardhi ambayo:

Kwanza: Makusudio ya Fardhi, yaani mwenye kusali hutakiwa kudhidhirisha kuwa ni mwenye kukusudia kusaliSala ya Fardhi;

Pili: Nia ya kusali, kumaanisha kuwa anaitaja aina yaSalah japo kwamjumuishowake na anakusudia kuitekeleza.Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wameichukulia Nia ya Salakua ni yenye kutofautisha Sala na vitendo vyenginevyo Kiibada.

Na ni lazima kuitamka nia ya Sala na kuendelea kua na nia hio kuanzaia mwanzo wa Sala hadi mwisho wa Sala, hivyo Mtu akibatilisha nia ya kuingia kwanye Sala wakati yumo kwenye Salam basi Sala yake hua ni batili pia.

Tatu: Nia ya kusali lazima idhihirishe Aina ya Sala husika yaani kwa mfano Sala ya Adhuhuri, au Al Asr, n.k.

Nne: Kua Nia ya Sala ni lazima iwe inaenda sambamba na *Takbirat A Ihram*

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: Nia ya Sala lazima iwe makhsusi kukumbuka aina ya Sala husika kwa Jina kwa mfano, Salat AdhDhur, Al Asr, Maghrib n.k

Na mbali ya kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanakubaliana kua Nia in lazima iambatane na Takbirat Al Ihram,lakini kwa upande wa Maimamwa Madhhab ya Imam Maliki, Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhhab yaImam Ahmad Ibn Hanbali, basi wao wanakubaliana kua ni sahihi kwa Nia kua ni yenye kuitangulia Takbirat al Ihram kwa muda mfupi.

Ama kuhusiana na Nia ya Salah za Qadha basi maelezo yake kulingana na Madhhab ni kama ifuatavyo:

Hua inapendekezwa Kutamka Nia kwa Ulimi na kwa Moyo hivyo kama ikiwa Mtu atanuia ndani ya Moyo wake kua analipa Sala Dhuhr lakini kama atatamka kua ni Salat Al Asr basi hua hamna tatizo, na hii ni kwa sababu kutamka kwa Ulimi hua si Kutia nia bali hua nikuthibitisha Nia iliyomo ndain ya Moyo, hivyo kasoro ya kuteleza kwa Ulimi hua hakuathiri kile kilichomo ndani ya Moyo, na huo hua ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, ambapo kwa upande wa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Abu Hanifa

Ama kuhusiana na Nia ya Salah za Sunnah basi maelezo yake kulingana na Madhhab ni kama ifuatavyo:

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wao wanasema kua:‘Sio sharti kubainisha Sala ya Sunna kua ni Sunna au la. Bali inatosha kukusudia kusali Sala kwa ujumla, isipokuwa ni kutahadhari zaidi katika Sunnah kukusudia Sala ya kumfuata *Rasul Allah Sala Allahu A’alayhi wa Salam*.

Vile vile ni hadhari zaidi katika Salah ya Tarawih kukusudia Tarawih, au Sunnah ya wakati huo, au sala ya usiku. Akikuta kundi linasali na hajui kuwa wanasali Tarawih au Salah ya Fardhi , na akataka kusali pamoja nao, basi atarajie Sala ya Fardhi. Ikidhihirika kuwa wanasaliSala ya Fardhi, inamtosheleza. Ikidhihirika kuwa wanasali Tarawiyh, Salah yake ni sahihi.

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Hanbali wanasema: ni sharti kubainisha Sunnah za kawaida kwa kukusudia Sunna ya Asr au Dhuhr, kwani ni sharti kubainisha Sunna ya Tarawih. Ama kuhusu Sala ya Sunnahkabisa, si lazima kukusudia kuibainisha, bali inatosha kukusudia Salah ya ukamilifu.

Wanazuoni wa Madhhab ya ImamAl Shafii wanasema: Sala ya Sunnahima ina muda maalumu, mfano wa Sunnah za kawaida na sala ya Dhuha, au haina muda maalumu, bali ina sababu, mfano sala ya Istisqa; au ni maombi ya hiari kabisa. Ikiwa ina wakati maalum au sababu, basi ni muhimu kuikusudia na kuibainisha, kwa kukusudia Sunnah ya Dhuhr, kwa mfano, na kwamba ni kabla au baada yake. Nia na uteuzi lazima pia viwiane na sehemu yoyote ya Takbir, na hii ndiyo maana ya ulinganisho wa kawaida na ukumbusho, na kitu kama hicho kimetajwa katika sala ya Fardhi, na nia ya Sala ya Sunna haihitajiki ila hua inapendekezwa, lakini ikiwa ni Sala ya Sunna, basi nia kamili ya sala inatosha ndani yake wakati wa kutamka sehemu yoyote ya sala. Takbira, na kubainisha hakutakiwi ndani yake, wala nia ya Sala ya hiyari, na kila Sala ya Sunnah yenye sababu inajumuishwa katika Sala ya Sunna. Hata hivyo, jambo jengine linatosha, kama vile Sunnah ya maamkizi ya msikiti, ambayo ni Sunna yenye sababu, ni kuingia msikitini, lakini inasaliwa ndani ya Sala yoyote inayoanzishwa baada ya kuingia msikitini.

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanasema: Salah isiyokuwa ya Fardhi ima ni Sunna iliyothibiti, nayo ni Sala ya Witr, Sala ya Idi mbili, Sala ya kupatwa kwa Jua na Istisqa, na haya lazima yabainishwe katika nia kwa kukusudia Salah ya Witr au Idi, na kadhalika; au ni ya kutamanika; Ni Salah ya Alfajiri na si kitu kingine, na pia inatakiwa kubainisha, kwa kukusudia kusali Alfajiri, au inapendekezwa, kama vile Salah za Sunnah, Duha, Tarawih na Tahajjud, na katika hali hii inatosha kusali. kuwa na nia kamili kwa ajili ya Sala, na wala haitakiwi kuibainisha, kwa sababu muda unatosha kuibainisha.

Takbirat Al Ihram, kwamba kama atamaliza Takbirat Al Ihram bila nia, ni batili.

Na kwa Upande wa Madhhab ya Hanafi wanasema: Ni sahihi kwa nia ya kutanguliza Takbirat Al Ihram, kwa sharti hakuna utengano baina yao ambao ni wa kigeni katika Sala, kama vile kula, kunywa au kuzungumza kunakobatilisha Sala. Ama kutengana kwa Salah, kama kuiendea au kutawadha, haidhuru.

Basi ikiwa alikusudia kusali Dhuhr, kwa mfano, akaanza kutawadha, na baada ya kumaliza akatembea hadi msikitini na kuanza kusali bila ya nia, basi Sala yake ni sahihi.

Umejifunza kutokana na yaliyotangulia kwamba makusudio ni mapenzi ya kuomba kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee. Bila ya kumshirikisha katika hilo jambo lolote la kidunia hata kidogo, basi alipokusudia hili, na akaianza Salah bila ya kutenganisha nia yake nayo kwa kitendo cha kigeni, basi atakuwa amefanya yale yanayotakiwa kwake, hivyo ikiwa alianza Sala na nia hii sahihi, basi mtu akamuingia, na akarefusha Salah ya kumsifu, basi hilo halibatilishi Salah, lakini hana malipo ya kurefusha huku, bali ana malipo ya Sala ya asili, kwa sababu nia wkwani kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*, na hii ndiyo maana ya kauli ya baadhi ya Hanafi; kwamba sala haiingii katika unafiki; wanamaanisha kuwa nia safi inatosha kwa usahihi wa sala; na unafiki wa kutokea haudhuru, ingawa ni uovu usio na manufaa kwa maafikiano. Je, nia ya kusali ni sahihi kabla ya wakati wake, kama vile akikusudia kusali, na kutawadha muda mfupi kabla ya muda kuanza, kisha akaenda msikitini bila ya kusema maneno ya kigeni, na akae humo mpaka muda utakapoanza na kusali? Jibu ni:

Lililopokewa kutoka kwa Abu Hanifa ni kuwa makusudio hayawi sahihi kabla ya muda kuanza, na baadhi yao wanasema: Bali ni sahihi kwa sababu nia ni sharti na sharti inatangulia sharti, kwa hiyo nia inatangulia. kwa asili. Wanachuoni wa Hanafi wameafikiana kuwa ni bora nia ifanywe wakati mmoja na takbira ya ufunguzi bila ya usumbufu wowote. Waigaji wa Hanafi wanapaswa kuzingatia hili na wasitenganishe takbirat na nia, kwa sababu ni bora na huondoa mgongano.

Hanbali wanasema: Nia inaweza kufanywa kidogo kabla ya takbira ya ufunguzi, kwa sharti kwamba atakusudia baada ya muda kuanza, kama ilivyoripotiwa kutoka kwa Abu Hanifa. Akikusudia kusali kabla ya wakati, nia yake haiwi sawa, kwa sababu nia ni sharti, kwa hivyo haidhuru ikiwa itatangulia Salah kama wasemavyo Mahanafi. Hata hivyo, Mahanbali wanasema: Lugha ya kigeni haikatishi nia. Akikusudia kusali basi aseme kitu nje ya Salakisha aseme takbira Sala yake ni sahihi. Waliweka nia tu kabla ya muda kuanza, kwa kuzingatia kutokukubaliana kwa wale wanaosema kuwa ni nguzo.

Hili, na ni bora kwao nia ifanywe kwa wakati mmoja na takbira ya ufunguzi, kama wanavyosema Mahanafi. Maliki walisema: Nia inaweza kufanywa kabla ya Takbirat Al Ihram kwa muda mfupi, kwa mujibu wa desturi, kana kwamba amekusudia mahali karibu na msikiti, kisha akasema Takbir msikitini, akisahau nia.

2-TAHARRUM - TAKBIRAT AL IHRAM

❖❖❖❖

Tunapozungumzia kuhusiana na Taharrum yaani Kuharamisha kila kitu kisichokua ni miogoni mwa Ibada ya kumuuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua tunazungumzia kuhusiana na kuingia ndani ya Sala kwa Takbir ya mwanzo ya Kuingia kwenye Sala ambayo hua unajulikana kama *Takbirat Al Ihram*. Na Hivyo Nguzo ya pili ya Sala baada ya Nia basi hua ni hii *Takbir Al Ihram* ambayo hua ni Kuelekea Kibla na kusema *Allahu Akbar*.

Ambapo bile ya Shaka kula mmoja wetu ni mwenye kujua maana ya Takbir yaani kumtukuza *Allah Subhabah wa Ta'ala* kwa kupitia katika Sifa yake Tukufu ya Kua na Ukubwa juu ya Kila Kitu usiofikirika wala usiokua na kifani.

Ama kuhusiana na neno *Ihram* basi limetokana na neno *Harama* ambalo humaanisha Kuharamisha, Kuzuia, Kukataza, Kuingiza kitu ndani ya Mipaka fulani na pia humaanisha Kukifanya Kitu kua kitukufu.

Ambapo Miji ya Makkah na Madina hua inaitwa *Al Haramayn* kwa sababu ya Utukufu wake na hivyo kumaanisha Sehemu Mbili Takatifu.

Hivyo Neno *Ihram* ambalo mara nyingi hua linatumika katika Kipindi cha Ibada ya Hija au Umra na hua linamaanisha kuingia katika hali Maalum Takatifu kwa Kuvaa nguo maalum za Vitambaa viwili visizoshonwa ambapo baada ya kuingia ndani ya nguo hizo basi kuna mambo ambayo mbali ya kua ni ya Halali Kisharia lakini hua hayaruhusiki kufanywa kutokana na kua mtu husika tayari ameshaingia katika hali ya Ihram kwa ajili ya kutekeleza Ibada Tukufu ya Hija au Umra.

Hivyo basi tunapozungumzia kuhusiana na Ibada ya Sala, basi Nguzo ya Pili imeitwa *Takbirat Al Ihram* kwa sababu ya kua Kitendo cha kutamka Allahu Akbar yenye sifa ya Takbirat Ihram hua kinamaanisha Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Sifa ya Ukubwa wake wa juu ya kila kitu, na kuthibitisha kua unaingia mbele ya Hadhara ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa ajili ya Kumuabudu na hivyo unaachana na mawazo na vitendo vyote visivyohusiana na Ibada yako hio ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani kwa wakati huo basi maneno na vitendo na vyengine vyote visivyohusiana na Ibada husika hua ni Haram.

Kwani *Takbira Al Ihram* hua pia inajulikana kama *Takbirat Al Iftitah* yaani Takbir ya Kufungulia Sala yaani ya Kuanzia Kuingia ndani ya Mipaka ya sala hivyo inabidi kuzingatia kua Kila Unaposema Allahu Akbar na Kuanza Kusali basi unatakiwa Ujihisi kua umetekeleza Nguzo ya pili ya Sala na Hivyo umejihudhurisha mbele ya Ukubwa wa Mola wako unaemuabudu.

Takbir Al Ihram hua ni Nguzo ya pili kwa Sababu tunapozungumzia Ibada ya Sala basi hua ni Ibada ambayo mbali ya kua tunatakiwa tuifanye huku tukiwa tumesimama. Lakini pia kama haiwezekani kusimama kutokana na Dharura basi tunatakiwa Kukaa, na kama haiwezekani basi hata kwa kulala kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Hadith ifuatayo katika Sahih Bukhari isemayo:

'Imran Ibn Husein *Radhi Allahu Anhu* anasema kua

كَانَتْ بي بَوَاسِيرُ، فَسَأَلْتُ النبيَّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ عَنِ الصَّلَاةِ، فَقالَ: صَلِّ قَائِمًا، فإنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَقَاعِدًا، فإنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَعَلَى جَنْبٍ.

Nilikua naumwa na Maradhi ya Bawasili na Hivyo nikamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Kusali, ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema:Sali ukiwa umesimama, na kama huwezi basi Sali ukiwa Umekaa, na kama huwezi basi Sali ukiwa umelalia Ubavu mmoja'*(Sahih Bukhari)*

Na pia Imam Ahmad Ibn hanbal amesema kua:

حَدَّثَنَا سُوَيْدُ بْنُ سَعِيدٍ، حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ مُسْهِرٍ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ، طَرِيفٍ السَّعْدِيِّ ح وَحَدَّثَنَا أَبُو كُرَيْبٍ، مُحَمَّدُ بْنُ الْعَلاَءِ حَدَّثَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ السَّعْدِيِّ، عَنْ أَبِي نَضْرَةَ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ، عَنِ النَّبِيِّ ـ صلى الله عليه وسلم ـ قَالَ " مِفْتَاحُ الصَّلاَةِ الطُّهُورُ وَتَحْرِيمُهَا التَّكْبِيرُ وَتَحْلِيلُهَا التَّسْلِيمُ "

Amesema Suwaidu Ibn Said kua amesema Aliyyu Ibn Mus-hir kua amesema Abi Sufyan kua amesema Taririf Ibn Saidi kua amesema Abi Nadhrat kua amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Ufunguo wa Sala ni Udhu, Kuingia ndani yake ni kwa Allahu Akbar na kuifunga kwake ni kwa Salam*(Sunnan At Tirmidhii, Sunnan Abu Daud,Musnad Imam Ahmad)*

Hivyo Hadith mbili hizi ambazo ni Sahih ni zenye kuainisha mpangilio wa Nguzo mbili za mwanzo za Sala ambazo ni Nia nakisha *Takbir Al Ihram.*

Ambazo hakuna njia ya kuziepuka kwa kisingizio chochote lakini kaa upande wa Kusimama ndio nguzo ya tatu kama tutakavyoona hapo baadae Inshaa Allah, Basi unaweza kukuepuka kutokana na kisingizio kinachokubalika kama ilivyosema Hadith ya Imran Ibn Husein *Radhi Allahu Anhu* alipokua akiumwa na Bawasili.

Ama kwa upande mwengine basi anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliingia Msikitini, na kisha kuna mtu akafuata kuingia baada yake na kisha Akasali na baada ya hapo akamsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Mtu huyo, kua: Nenda Kasali tena.

Kwani kwa hakika wewe hukusali.

Hivyo Mtu huyo akarudi na akasali tena kisha akarudi *kwa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumsalimia tena.

Lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuambia tena mtu huyo kua: Nenda Kasali Tena kwani kwa Hakika wewe hukusali.

Hivyo mtu huyo akarudia tena Kusali, na hali hio ikajirudia mara tatu, na ilipofika mara ya nne basi akasema kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ya Rasul Allah, Naapa mimi kwa yule ambae Roho yangu iko mikononi mwake kua kwa hakika mimi siwezi kusali kwa njia bora zaidi ya hivi nnavyojua. Hivyo basi bora nifundishe.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Unaposimama Kusali basi sema Takbir, Kisha Soma kutoka katika Quran kile unachokijua kwa Moyo. Kisha Rukuu hadi uwe umetulia, kisha Nyanyua Kichwa chako na Usimame sawia, kisha Usjudu hadi uwe umepata utulivu ndani ya Sijda yako, na kisha kaa Kitako hadi upate utulivu na fanya hivyo katika kila Sala yako.'** *(Sahih Bukhari)*

Hivyo Nia ya Sala ni lazima iambatane na Takbir Al Ihram. Kwani ni kama*alivyosema Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam*katika hadith ifuatayo:

حَدَّثَنَا سُوَيْدُ بْنُ سَعِيدٍ، حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ مُسْهِرٍ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ، طَرِيفٍ السَّعْدِيِّ ح وَحَدَّثَنَا أَبُو كُرَيْبٍ، مُحَمَّدُ بْنُ الْعَلاَءِ حَدَّثَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ السَّعْدِيِّ، عَنْ أَبِي نَضْرَةَ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ، عَنِ النَّبِيِّ ـ صلى الله عليه وسلم ـ قَالَ " مِفْتَاحُ الصَّلاَةِ الطُّهُورُ وَتَحْرِيمُهَا التَّكْبِيرُ وَتَحْلِيلُهَا التَّسْلِيمُ "

Amesema Suwaidu Ibn Said kua amesema Aliyyu Ibn Mus-hir kua amesema Abi Sufyan kua amesema Taririf Ibn Saidi kua amesema Abi Nadhrat kua amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Ufunguo wa Sala ni Udhu, Kuingia ndani yake ni kwa Allahu Akbar na kuifunga kwake ni kwa Salam*(*Sunnan At Tirmidhii, Sunnan Abu Daud,Musnad Imam Ahmad)*

Kwa maana hio basi Mtu yeyote asiesema Takbir Al Ihram iwe kwa Kusahau, kwa kutojua kua huo ndio Ufunguo wa Sala basi Sala yake hua haikubaliki na itambidi aianze tena upya Sala yake hio.

Hivyo kama Mtu ikiwa ana hali ya shaka yaani hana uhakika kama alisema *Allahu Akbar* ama la au labda atakua amekumbuka ndani ya Sala kua kumbe hakuanza na *Takbir Al Ihram* basi Mtu huyo

anatakiwa aanze Upya Sala yake hio katika wakati huo huo kwani ukweli ni Kua katika hali kama hio hua hahesabiki kua yuko ndani ya Sala.

MASHART YA TAHARRUM - TAKBIRAT AL IHRAM

Tunapozungumzia *Takbir Al Ihram* basi ni lazima pia itamkwe kama inavyotakiwa yaani Allahu Akbar, ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wanasema kua Takbirat Al Ihram inaweza kutamkwa kama *Allahu Akbar! Au Allahu Al Akbar!* Kwa sababu Hadith imetumia neno *Al Takbir,* ambapo *neno Al* hua ni lenye kuonesha *Hukm* ambayo inashikamana na kitu kilichoelezewa na si zaidi ya kitu husika.

Imam Al Shafii anasema kua: **'Na haitoshelezi kwa mtu kua ni menye kuingia ndani ya Sala kwa Moyo wake tu au kwa kusoma kwa Moyo wake, bali anatakiwa awe ni mwenye kuuchezesha ulimi wake katika kutamka kwake.'**

Ingawa kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi kuhusiana na Takbirat Al Ihram tunaona ni kua na: **'Takbira Al Ihram hua inatakiwa itamkwe wazi kwa wale watu wenye uwezo wa kuitamka kwa kiasi ya kua mtamkaji awe ni mwenye kuisikia yeye mwenyewe.'***(Al Muta'amad fi Al Fiqh Al Shafii)*

Na neno Akbar la*Takbirat Al Ihram* lisiwe linatamkwa kwa kuvuta kama **Allahu Aaakbar** au **Allahu Akbaar** na wala isiwe ni yenye kuonesha tofauti baina ya maneno yake mawili yaani **Allahu……..Akbar** n.k

Kwani kufanya hivyo hua ni kubadilisha maana ya *Takbir Al Ihram.*Na hivyo haikubaliki kutumia lugha nyengine wala neno jengine badala yake kwa mfano labda

سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ وَلاَ حَوْلَ وَلاَ قُوَّةَ إِلاَّ بِاللَّ

Subhanah Allah, au Alhamd lillah au La Hawla wa Quwwata illa bi Allah. n.k.

Lakini kwa upande wa Imam Abu Hanifa na Imam Muhamamd Ash Shaybani basi wanasema kua: **'Inakubalika kutamka Takbir al Ihram hata kwa maneno yenye kumaanisha maana moja na Allahu Akbar yaani kwa mfano Allah Al Adham! Au Allahu Al Aajal ambayo yote maana yake hua ni Allahu Akbar.'**

Na pia kwa upande wa Imam Abu Yusuf ambae ni Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa basi yeye anasema kua: **'Takbir al Ihram inayokubalika ni *Allahu Akbar* tu.'***(Mukhtasar Al Quduri)*

Na anasema Imam Al Sayyid Al Bakri Al Dimyati Al Shafii kua: '**Masharti ya Takbirat Al Ihram ni:**

1- **Mwenye Kusali anyanyue sauti yake katika kuitamka kwake hadi yeye mwenyewe asikie Herufi zake zote, bila ya kuwepo kwa kizuizikatika maneno yake.**
2- **Mwenye Kusali anatakiwa awe katika hali ya Kusimama ambako ni Wajibu katika Sala.**
3- **Lazima itamkwe kwa Lugha ya Kiarabu kama ikiwa mtu anaesali anaweza kuitamka na kuiweka katika maneno yake.**
4- **Inapaswa itamkwepamoja maneno yote *Allahu Akbar.***
5- **Inapaswa kwa neno Allahu kupewa kipaumbele zaidi kimpangilio katika kutamka kuliko neno Akbar.**
6- **Haitakiwi kuivuta Alif Hamza katika neno Allahu, kwani kunabadilisha maana na kuifanya kua ni yenye kuhoji badala ya kuthibtisha.**

7- **Haitakiwi kuivuta Herufi Ba katika neno Akbar kwa kuweka Alif baada yake kwani kunabadilisha maana.**
8- **Haitakiwi kuitia Shadda herufi Ba katika neno Akbar.**
9- **Haitakiwi kua na pumziko la kukaa kimya baina ya neno Allahu, ila kama itakua ni pumziko linalotokana na kutaka kupumua basi hamna tatizo, na haidhuru kusema *Allahu Al Akbar au kusema Allah Al Adhimu Akbar!***
10- **Neno Allahu lisivutwe zaidi ya Harka 14.**
11- **Haitakiwi kua na pumziko, au katisho au kimya baina ya Maneno mawili haya Allahu Akbar.**
12- **Kusiwe na Herufi Waw baina ya Maneno mawili haya Allahu na Akbar.**
13- **Iwe ni katika Mda wa kuingia kwenye Sala ya Fardhi au Sunna na kwa sababu hio.**
14- **Itamkwe wakati Mtu akiwa ameelekea Kibla.**
15- **Kutoichelewesha Takbir Al Ihram baada ya Nia, yaani itamkwe mara tu baada ya kutiwa nia ndani ya Moyo na kutamkwa kwa nia.**
16- **Isiitangulie Takbirat Al Ihram ya Imam katika Sala ya Jamaa na wala isiende sambamba na Takbira Al Ihram ya Imam.**
17- **Iwe na Mvutio wa Sauti inayokubalika katika kutamkwa.**
18- **Itamkwe kwa herufi zake zote bila kua na haliya kusitishwa au kuachwa hata herufi moja baina yake.**
19- **Iwe ni kwa ajili ya kuingilia ndani ya Sala na isiwe kwa ajili nyengine yeyote, yaani isiwe ni kwa ajili ya Takbirat Al Itiqaal (Takbirat ya kuhama kutoka na kuingia katika vituo tofauti vya Sala) pia.**
20- **Kuikata Hamza katika Neno Akbar na kuifanya herufi hio kua ni Hamza ya Asli ya kuunganisha basi hua haikubaliki na wala kuweka herufi waw katika neno Akbar kwa kutamka Wakbar, isipokua kwa Mtu asiejua ambae hua ni mwenye kusamehewa juu ya kosa hilo.** (*Nail Al Raja' Fi Sharh Safinat Al Naja*)

Anasema Imam Al Qalyubi kua: **'Kama Imam atakua ni mwenye kukosea katika wakati wa kutamka Takbirat Al Ihram, kukosea ambako hakutobadilisha maana ya Takbir, basi Sala husika itakua Sahih, kwani kukosea kidogo hua hakubatilishi Sala'**(*Hashiah Al Qalyubi 'Ala Sharh Al Muhalla 'Ala Minhaj Al Talibin*)

Ambapo kwa upande wa Al Muhaqqiq Imam Ibn Hajar Al Haythami basi yeye anasema kua: **'Kama ikiwa Imam anakasoro ya Lafdhi ya uzito katika Ulimi wake na hivyo akawa hawezi kutamka herufi Ra labda kwa mfano basi hua hamna tatizo na Sala yake hua ni Sahih lakini iwe imetamkwa kwa njia sawia kisautihata kama ikiwa haisikiki vizuri'**(*Tuhfah Al Minhaj Bi Sharh Al Minhaj* , 7/295).

Lakini kama ikiwa Mtu atakua ni mwenye kukosea kukubwa sana kiasi ya kua kukosea kwake kutabadilisha maana katika utamka kwa mfano herufi Alif ikivutwa katika kutamka Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hapa itakua inabatilisha Sala na hii ni kwa sababu Alif inapovutwa hua ni yenye kuonesha hali ya kuhoji badala ya kuthibitisha na hivyo kua ni yenye kumaanisha kua kuna shaka juu juu ya kinachotamkwa.

Anasema Imam Al Muhaqqiqin Al Faqih Imam Ibn Hajar Al Haythami Al Shafii kua : **'Kama Mtu atakua na Ulimi mzito kwa mfano katika kutamka baadhi ya herufi, kwa mfano Ra basi hua**

hamna tatizo kwani Sala yake hua Sahih lakini kwa sharti la kua iwe ni yenye kutamkwa kwa kutumia njia sahih ya kutokea kwa maneno katika kinywa hata kama itakua tamko la herufi hio haliko wazi'

kwa maana hio basi kama katika utamkwaji wa *Takbirat Al Ihram* kama Mtu atakua ana tatizo katika Ulimi wake kimatamshi, basi hii hua haibatilishi Sala yake. Lakini kama ikiwa tamko la herufi husika linaonesha wazi kua ni lenye kubadilisha maana husika iliyokusudiwa kama tulivyoona katika kuivuta Alif ya Allah basi hili litakua ni tatizo ambalo litapelekea kua ni kosa kubwa.

Kwani anasema Al Khatib Al Shirbini kua**: 'Hairuhusiki kuivuta Herufi Alif katika kulitamka jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* .**'*(Al Iqna Fi Hilli Alfaz Abi Shujaa)*

Na anasema Imam Muhammad An Nawawi Al Jawi Al Bantani Al Shafii kua: **'Kama Alif katika neno Allah itavutwa basi itabadilisha mfumo kamili wa neno kutoka katika K*habar Insha'I* na kuliingiaza kwenye *Istifham,* na hivyo kupelekea kuingia kwenye Kufuru kwani hua ni kwenye kuhoji uwepo wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* .'***(Kashfiyah Al Saja Sharh Safinat Al Naja)***

Kwa maana hio basi ndio maana inasisitizwa kwa Waislam hususan Maimam wanaosalisha kua ni wenye kutakiwa kujifunza na kuijua Lugha ya Kiarabu kwani kufanya hivyo hua ni kwnye kupelekea katika kujua kuhusiana na Ilm ya Dini ya kiislam na Hukmu zake katika Ibada.

Kwani amesema Abu Masud Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* kua:

يَؤُمُّ الْقَوْمَ أَقْرَؤُهُمْ لِكِتَابِ اللَّهِ فَإِنْ كَانُوا فِي الْقِرَاءَةِ سَوَاءً فَأَعْلَمُهُمْ بِالسُّنَّةِ

'Watakaokua Maimam katika Ummah wangu ni wale ambao ni wenye Ufahamu wa Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* , na kama wote wakiwa sawa basi atakaekua Imam ni Yule Mwenye Ilm zaidi ya Sunna zangu.'*(Imam Muslim)*

Na *Takbirat Al Ihram* hua inatakiwa kutamkwa nia ya mara moja, kwa maana hio basi kama ikitamkwa kwa nia ya zaidi ya mara moja, basi Takbir zitakazofuatia hua ni zenye kubatilisha Sala husika.

Kwani amesema *Shaykh Ul Islami* Imam Abu Zakariyyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: **'Kama ikiwa mtu atafanya *Takbir*kwa nia ya *Al Ihram*na kisha akafanya *Takbir Al Ihram* mara nyengine zaidi basi hua ni mwenye kuingia kwenye Sala ya Witri ambayo hua imebatilishwa na sala ya Shafaa na hivyo hua ni mwenye kuingia kwenye Sala kwa kila *Takbir al Ihram* ya kuifungulia Sala na kisha hua si mwenye kukusudia kutoka kwenye Sala hio bali hua ni mwenye kuingia kwenye Sala nyengine ndani yake. Hivyo Sala yake hubatilika kwa sababu ndaniyake hua inajumuisho la batilisho la Sala ya kwanza.'***(Majmuu Sharh Muhadhdhab)***

Na kwa upande wa Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shibrini Al Khatib Al Shafii basi anasema kua: **'Kama ikiwa Mtu atafanya *Takbir Al Ihram* kadhaa kwa nia ya kuingia ndani ya Sala kutokana nazo basi hua ni mwenye kuingia ndani ya Sala kwa *Takbir* ya kwanza na kutoka ndani ya Sala kwa *Takbir* ya pili, kwani mwenye kuanza Sala na kisha akanuia Sala nyengine basi hua ni mwenye kuibatilisha Sala yake.'**

Na Imam Al Ramli anasema kua: **'Kama mtu akisema Allahu Akbar katika hali ya Ihram, na kisha akasema tena kwa nia ya Ihram tena basi hua ni mwenye kuingia ndani ya Sala kwa njia ya Witr na kutoka kwa njia ya Shafaa.'**(*Nihayah Al Muhtaj Ila Sharh Al Minhaj*)

Ambapo hata hivyo kama ikiwa Mtu atakua na nia ya Takbir ya kwanza tu, na kisha Takbirat ya pili ataitamka bila ya bila ya kua na Nia ya kuingia ndani ya Sala, bali kwa nia ya Dhikr Allah basi kufanya hivyo hua hakubatilishi Sala husika, kama anavyosema Imam An Nawawi tena kua: '**Na kama mtu ikiwa hakutamka Takbir ya pili na itakayofuatia kwa nia ya kuingia ndani ya Sala, basi Sala yake itakua ni Sahih kutokana na kua Takbir ya Kwanza kua ni *Takbir ya Ihram* na Takbir ya pili kua ni kama dhikr**'(*Al Majmu' Sharh Al Muhazzab*)

Ambapo huo pia ndio mtizamo wa Imam Al Ramli katika ***Nihayah Al Muhtaj Ila Sharh Al Minhaj***, 4/68 pale aliposema**: 'Kama Mtu atakua na nia ya kuingia ndani ya Sala kwa Takbir Al Ihram na kisha akatamka Takbir nyengine bila ya kua na nia ya Ihram basi kufanya hivyo hakutoiathiri Sala yake.'**

RAF AL YADAIN

❖❖❖

Na mbali ya kutamka maneno ya Takbir Al Ihram, lakini pia katika wakati wa kusema Allahu Akbar basi Mtu anatakiwa kunyanyua viganja vya Mikono yake kufikia katika usawa wa Mabega yake au juu zaidi karibu kuyafikia na Masikio, na hiki ni kitendo ambacho kinajulikana kama R*af Al Yadayn.*

Yaani *Takbir Al Ihram* hua inaenda sambamba na *Raf Al Yadayn* - yaani Kunyanyua Mikono katika wakati wa kusema Allahu Akbar.

Ambapo amesema Imam An Nasai kua:

خْبَرَنَا سُوَيْدُ بْنُ نَصْرٍ، قَالَ أَنْبَأَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ الْمُبَارَكِ، عَنْ قَيْسِ بْنِ سُلَيْمٍ الْعَنْبَرِيِّ، قَالَ حَدَّثَنِي عَلْقَمَةُ بْنُ وَائِلٍ، قَالَ حَدَّثَنِي أَبِي قَالَ، صَلَّيْتُ خَلْفَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَرَأَيْتُهُ يَرْفَعُ يَدَيْهِ إِذَا افْتَتَحَ الصَّلاَةَ وَإِذَا رَكَعَ وَإِذَا قَالَ " سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ " . هَكَذَا وَأَشَارَ قَيْسٌ إِلَى نَحْوِ الأُذُنَيْنِ.

Amesema Suwayd Ibn Nasr kua amesema: Abdullah Ibn Al Mubarak kua amesema:Qais Ibn Sulaym Al Anbari, kua amesema: Alqamah Ibn Wa'il kua: Amenihadithia Baba yangukua: 'Nilisali mimi nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*na nilimwona akinyanyua Mikono yake Alipoingia kwenye Sala, na (alikua akinyanyua mikono) aliporukuu, na (alikua akinyanyua mikono) aliposema: "Sami Allahu Liman hamida". Hivyo ndivyo Qais alivyoashiria kuelekea kwenye Masikio yake.*(Sunan An Nasai)***

Hivyo kuna Ijmaa au Makubaliano ya Masahaba, Tabiina, Tabii Tabiina na Wanazuoni juu ya *Raf Al Yadayn* katika wakati wa *Takbir Al Ihram.*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Hadith za *Raf Al Adayn* zimenukuliwa nyingi sana kutoka kwa Masahaba kiasi ya kua hakuna hadith nyenginezo zilizonukuliwa kwa wingi zaidi kuliko Hadith za *Raf Al Yadayn'*.**

Na amesema Mujaddid Ad din Shaykh Ul Islami Al Hafidh Imam Shihab Ad Din Abu Fadhil Ahmad Ibn Nur Ad Din Ibn Ali Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani kua: '**Amesema Imam Al Hakim kua: Hakika sisi hatujui Sunnah yeyote ile isipokua *Raf Al Yadayn* ambayo juu yake imekubaliwa na Makhalifa wote wanne *Radhi Allahu Anhum,* Masahaba kumi *Radhi Allahu Anhum,* walioahidiwa Pepo na Masahaba wengine *Radhi Allahu Anhum,* wengi Sana hadi wale waliohamia katika Ardhi za Nchi Nyengine Tofauti *Radhi Allahu Anhum*.***(Fath Barr)***

Na kwa upande wa Imam Abu Bakr Ahmad Ibn Husein Ibn Ali Ibn Musa Al Bayhaqi basi yeye amenukuu Hadith za Masahaba 50 wasemao kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifanya *Raf Al Yadayn* katika wakati wa Takbir Al Ihram.

Kwani anasema Shah Waliyu Allahu Al Dahlawi Al Hanafi kua:'**Mtu anaenyanyua Mikono yake katika Takbir Al Ihram ni mwenye Kupendwa zaidi kwangu mimi na hii ni kwa sababu Hadith za *Raf Al Yadayn* ni nyingi sana na ni Sahih.'**

Na akasema Shaykh Anwar Al Kashmir kua: **'Kwa msingi wa Maneno ya Hadith na Sanad za Hadith na vitendo vyake basi Hadith za Raf Al Yadayn ni Mutawwatir, zisizokua na shaka ndani yake.'**

Ambapo miongoni mwa Hadith hizo ni pamoja na ile ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* isemayo: **Wakati R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akitamka *Takbir Al Ihram* basi alikua akinyanyua viganja vya mikono yake kukabiliana na mabega yake.Na anaporukuu hufanya hivyo pia, na anaponyanyuka kutoka kwenye Rukuu kwa ajili ya kuelekea kwenye Sujud basi hufanya hivyo.Na anaponyanyuka katika Rakaa mbili za Mwisho (yaani baada ya Attahiyat ya pili)hufanya hivyo pia.'**(*Imam Abu Daud)*

Na akasema Imam An Nafii ambae ni Mwanafunzi wa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **Kila wakati ambao Ibn *Umar Radhi Allahu Anhu,* alipokua akianza Sala yake kwa *Takbir Al Ihram* basi alikua akinyanyua mikono yake. Na kila anaporukuu basi alikua akinyanyua mikono yake na pale anaponyanyuka na kusema *Sami Allahu Liman Hamida* hunyanyua mikono yake.Na alikua akifanya hivyo pia katika kunyanyuka kuingia kwenye Rakaa ya tatuNa Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akisema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifanya hivyo pia.**

Kwani kwa upande mwengine basi amesema Wail Ibn Hujr *Radhi Allahu Anhu* kua:'**Mimi nilikua kwa makusudi nikiiangalia Sala ya *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam,* na namna alivyokua akisali.*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisimama kuelekea Kibla na kusema Allahu Akbar, huku akinyanyua Viganja vya mikono yake hadi mbele ya masikio yake,na kisha anaishika mikono na kuuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto huku ikiwa imekamatana.**

Wakati anapotaka Kurukuu basi huinyanyua tena mikono yake kama hapo kabla na kisha huweka mikono yake magotini, na anaponyanyuka kutoka kwenye rukuu hunyanyua tena mikono kama hapo kabla na anaposjudu basi huliweka paji laki la uso baina ya mikono yake'*(Imam Abu Daud)*

Na amesema Imam Ibn Al Mundhiri al Nishapuri kua: **'Kuna makubaliano ya Ijmaa ya Wanazuoni kuhusiana na uhalali wa Sunnah ya kunyanyua mikono katika Sala.'**

Imam Ibn Hajar Al Asqallani anasema kua: **'Baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wamenukuu kutoka kwa Imam Abu Hanifa kua Mtu anaedharau kunyanyua mikono yake katika wakati wa kufunga Sala hua ni mwenye kufanya Dhambi'**

Na anasema Shyakh Ul Islami Taqid Ad Din Abu Fatah Muhamamd Ibn Ali Ibn Wahb Ibn Muti Ibn Abi Taa Ibn Daqiq Al Idd Al Shafii kua: '**Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii bas ni kua Inapendekezwa kunyanyua mikono kwa sababu kuna uthibitisho wa kunyanyuliwa kwa mikono katika wakati wa Kurukuu na kuinyanyua kwake hua ni kama kuinyanyua katika wakati wa mwanzo wa Sala na pia kuna vithibitisho katika kila sehemu zote ilizopendekewa kuinyanyua mikono, na pia imeridhiwa kutokana na wale waliokua wakifanaya hivyo hapo kabla**

katika vizazi vya mwanzoni. Na mtizamo uliokua sahih ni kua inapendekezwa kunyanyua mikono pale unaposimama kutoka katika ya pili kwa sababu sababu hadith zimethibitisha juu ya hilo'

Ambapo Imam An Nasai anasema tena kua:

أَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ مَسْعُودٍ، قَالَ حَدَّثَنَا يَزِيدُ، - وَهُوَ ابْنُ زُرَيْعٍ - قَالَ حَدَّثَنَا سَعِيدٌ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ نَصْرِ بْنِ عَاصِمٍ، أَنَّهُ حَدَّثَهُمْ عَنْ مَالِكِ بْنِ الْحُوَيْرِثِ، أَنَّهُ رَأَى رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَرْفَعُ يَدَيْهِ إِذَا رَكَعَ وَإِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ حَتَّى يُحَاذِيَ بِهِمَا فُرُوعَ أُذُنَيْهِ" .

Ismail Ibn Masoud amesema kua Yazid amesema kua - na yeye ni Ibn Zuray' - amesema kua Said amesema kua Qatada amesema kua, kutoka kwa Nasr Ibn Asim, amesema kua Malik Ibn Huwairith *Radhi Allahu Anhu* kua:'Kwa hakika alikua*Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam akinyanyua* mikono yake wakati alipokua akisali, akirukuu, akinyanyuka kutoka kwenye rukuu anapoelekea kwenye kusjudu na anapokuja juu kutoka kwenye Sujud, mikono yake hio ilikua ikifikia usawa wa juu ya sehemu ya masikio yake.'*(Sunan An Nasai)***

Hivyo kwa upande wa Imam basi hua ni Wajib kwake Kusema *Allahu Akbar* yaani *Takbir Al Ihram* kwa sauti ili kila anaemfuata Nyuma yake awe ni mwenye kumsikia ili nao wapate kusema *Takbir Al Ihram* yao kwa kila mmoja miongoni mwao.

Kwa maana hio basi Kama Imam hakusema *Allahu Akbar* iwe kwa makusudi au kusahau na akafunga Sala, na kisha walio nyuma yake wakamfuata bila ya kusikia akisema *Allahu Akbar* basi Imam huyo hana Sala wala Maamuma wake hawana Sala, na kama Imam akisema mara ya kwanza *Allahu Akbar* na kisha akasema tena na kunyayua mikono na kufunga Sala basi na Maamuma hutakiwa aseme tena *Allahu Akbar* kwa sababu huenda Imam alifanya hivyo kwa sababu mwanzoni alikosea katika Nia yake na akaamua kutia tena nia na kuanza upya Sala.

Yaani kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Zayn Ad Din Al Sunayki Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Masri Al Shafii kua: **'Hapa hua kuna hali ya kutakiwa kuacha kufanya kitu, kwa sababu ya hali yakuharibika kwa kitu ambacho uhalali wake haujathibitishwa na hivyo hakiwezi kufuatiliwa zaid ya vile kilivyotokea katika wakati husikakatika kutokea kwake. Yaani kwa mfano Imam ameingia ndani ya Sala na akanuia kusali Rakaa mbili badala ya Rakaa Nne na akafanya Takbrat al Ihram, na kisha akafanya tena Takbirat Al Ihram kwa mara ya pili kutokana na nia ya kusali Rakaa nne.**

Ambapo hali hii hapa pia hua tunaweza kusema kua hii inaweza ikabatilisha Sala kwa sababu ya kutokana na kutoikana Nia ya Kwanza na kuongezea Nia ya Pili Juu yake hivyo Nia ya kwanza hua ni batili na nia ya pili hua haikubaliki kwa upande mmoja lakini kwa upande wa pili basi nia ya pili hua inaweza ikakubalika kwa sababu nia ya pili hua ni nia ya Sala inayoendelea.'

Na *Takbir Al Ihram* hio hua inaambatanishwa na kitendo cha Raf Al Yadayn yaani kunyanyua Mikono aidha hadi viganja vikafika kwenye usawa wa mbele ya Mabega au vikafika karibu na Masikio, na hii ni kulingana na uthibitisho wa Hadith kadhaa pamoja na tulizoziangalia hapo kabla.

Hivyo Mtu anaweza akanyanyua mikono hadi mbele ya Mabega na mwengine akanyanyua hadi masikioni, hii hua haina tatizo kwani vyote hua ni sawa, kulingana na vithibitisho vya Hadith mbali mbali kama tulivyoona baadhi yao miongoni mwao.

Kwani kuna baadhi ya Wanazuoni wametafsiri kitendo cha *Raf Al Yadayn* kua ni sawa na kuondoa pazia baina ya Mja na Muumba wake anaemuabudu. Ambapo ingawa *Takbir Al Ihram* na *Raf Al Yadayn* hua ni vitendo vinavyotakiwa kutekelezwa wakati Mtu akiwa katika hali ya kusimama ambayo ni Nguzo ya hatua ambayo tutaielezea baadae.

Kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Zayn Ad Din Al Sunayki Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Masri Al Shafii kua: '**Hikma ya Imam kunyanyua mikono katika *Raf Al Yadayn* hua ni kutokana na kua hata kama kuna Viziwi miongoni mwa wau wanaosali basi wanaweza kuona Ishara hio na hivyo kua ni wenye kujua kua tayari Sala imeshaanza kusaliwa kama vile ambavyo Kipofu atakapojua kuanza kwa Sala kutokana na kusikia Sauti ya *Takbirat Al Ihram,* au kuashiria kuondoa Pazia baina ya Kiumbe na Muumba, au kusimama na kuangaliana kwa mkabiliano wamwili mzima na kama alivyosema Al Shafii kua kufanya hivyo hua ni Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kufuata Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Ama kwa upande mwengine basi amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali huku akiwa Safarini Juu ya Kipando chake (Farasi au Ngamia) kokote Kule kilikoelekea, alikua akiashiria hatua za Sala ya Usiku, isipokua Sala za Fardhi , na alikua akisali Witri Juu ya Kipando chake.'***(Sahih Bukhari na Muslim)*

Hivyo inaruhusika kwa Dharura kusali ukiwa umekaa Juu ya Kipando, ukiwa Safarini ukiwa Juu ya Farasi, Ngamia, kwenye Ndege, kwenye Treni, kwenye Meli n.k kama vile inavyoruhusika kusali kwa kukaa au kulala ukiwa unaumwa. Ambapo amesema pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

حَدَّثَنَا إِسْحَاقُ بْنُ مَنْصُورٍ ، قَالَ : أَخْبَرَنَا رَوْحُ بْنُ عُبَادَةَ ، أَخْبَرَنَا حُسَيْنٌ ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ بُرَيْدَةَ ، عَنْ عِمْرَانَ بْنِ حُصَيْنٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ : أَنَّهُ سَأَلَ نَبِيَّ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ، وَأَخْبَرَنَا إِسْحَاقُ ، قَالَ : أَخْبَرَنَا عَبْدُ الصَّمَدِ ، قَالَ : سَمِعْتُ أَبِي ، قَالَ : حَدَّثَنَا الحُسَيْنُ ، عَنْ ابْنِ بُرَيْدَةَ ، قَالَ : حَدَّثَنِي عِمْرَانُ بْنُ حُصَيْنٍ – وَكَانَ مَبْسُورًا – قَالَ : سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ صَلاَةِ الرَّجُلِ قَاعِدًا ، فَقَالَ : إِنْ صَلَّى قَائِمًا فَهُوَ أَفْضَلُ وَمَنْ صَلَّى قَاعِدًا ، فَلَهُ نِصْفُ أَجْرِ القَائِمِ ، وَمَنْ صَلَّى نَائِمًا ، فَلَهُ نِصْفُ أَجْرِ القَاعِدِ

Ishaq Ibn Mansour amesema kua Ruh Ibn Ubadah kua amesema Husein kua amesema Abdullah Ibn Buraidah, kua amesema Imran Ibn Husein Mungu *Radhi Allahu Anh*u kua Alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Ishaq akatufahamisha kua Abd Al Samad amesema Ibn Husayn – ambae alijibu kwa mchangamfu - kua: Nilimuuliza mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*juu ya Salah ya mtu aliekua amekaa, na akasema:'Yeyote yule atakaesali akiwa amesimama basi hua ni bora kwake, Akisali akiwa amekaa basi hupata Nusu ya Malipo ya aliesali kwa kusimama.'*(Imam Bukhari)***

Na Imam Muslim, Imam Abu Daud na Imam Al Nasai wana na Hadith isemayo:

عبد الله بن عمرو قال بلغني أن النبي – صلى الله عليه وسلم – قال : صلاة الرجل قاعدا على نصف الصلاة ، فأتيته فوجدته يصلي جالسا فوضع يدي على رأسي ، فقال : ما لك يا عبد الله ؟ فأخبرته فقال : أجل ، ولكني لست كأحد منكم .

Amesema Abd Allah Ibn Amr *Radhi Allahu Anhu* kua:'Niliambiwa mimi kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Sala ya Mtu aliekaa Kitako hua ni Nusu ya Sala ya Mtu aliesimama' hivyo nikamuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa anasali huku akiwa amekaa kitako, nami nikaweka mkono wangu juu ya kichwa chake. Ambapo nae akasema: Kuna Tatizo gani ewe Abd Allah Ibn Amr?'

Nami nikamwambia: 'Nimeambiwa ya *Rasul Allah! (Salallahuu Alayhi wa Salam)* kua umesema kua: ''Sala ya Mtu aliekaa Kitako hua ni Nusu ya Sala ya Mtu aliesimama' kisha nakuona kua unasali huku ukiwa umekaa kitako'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Naam, Ila mimi nitofauti na nyinyi.'(Sahih Muslim)*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din ImamAub Zakarriyah Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: **'Kilichomaanishwa hapa ni kua Sala ya Mtu aliekaa hua ni yenye Malipo ya Nusu kulingana naSala ya Mtu aliesimama, yaani Sala hio hua ni yenyekukubalika ila, hua ni yenye Malipo kidogo. Ambapo Hadith ii inatakiwa kuangaliwa kuingna na mtizamo wa Sala za Sunnah ambazo Mtu anaweza kuslai huku akiwa amekaa kitako wakati Mtu huyo akiwa ni mwenye kuweza kusiamama. Hivyo Malipo yake hua ni nusu ya Sala ya Mtu anaesimama.**

Lakini kwa mtu atakaesali Sala ya Sunna kwa sababu hawezi kusimama basi malipo yake hua hayapunguzwi na hua ni sawia na ya Sala ya Mtu aliesimama. Ama kuhusiana na Sala za Fardhi basi kama Mtu akisali kwa kukaa Kitako wakati anao uwezo wa kusimama, basi Sala ya Mtu huyo hua ni Batili, na hatolipwa chochote bali hua ni mwenye kufanya dhambi'

Ambapo As-hab wetu wamesema kua: 'Kama ikiwa Mtu ataamini kua kufanya hivyo hua kunaruhusika basi Mtu huyo hua si mwenye Kuamini na hua ni mwenye kustahiki kuingizwa katika hukmu ya miongni mwa watu waliotoka katika Uislam, kama vile ambavyo Mtu anaeamini kua Zinaa na Riba na mambo mengine yaliyokatazwa kua ni ni yenye kuruhusika.

Hivyo kama mtu akisali Sala ya Fardhi kwa kukaa kitako kwa sababu hawezi kusimama, au kwa kulala kwa sababu hawezi kukaa kitako, basi malipo yake yatakua ni sawa na yule aliesimama na wala hatopunguziwa na hii ni kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni. Ama kuhusiana na hadith ya kupunguziwa kwa Malipo basi inabidi kufahamike kua inawahusu wale wanaosali Sala za Sunna wakiwa wamekaa wakati wakiwa na uwezo wa kusimama. Na hivi ndivyo ilivyotofautishwa na Wanazuoni wetu kuhusiana na usahih wa Hadith hii.'

Na kuhusiana na kauli ya *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* aliposema kua: 'Mimi sio kama nyinyi' basi Wanazuoni wetu wanasema kua hii ni kulingana na upekee wa Darja na sifa zake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kua Sala zake za Sunnah anazozisali huku akiwa amekaa kitako hua ni sawa na Sala zake anazozisali huku akiwa amesimama kutokana na Utukufu wake, ambao umemtenganisha kama vile ulivyomtenganisha kwa mambo mengineyo ambayo wameyazungumzia As-hab wetu na wengineo kama tulivyofafanua katia Asma wa Lughat.' *(Sharh Sahih Muslim)*

Na kwa kua Raf Al Yadayn - Kunyanyua Mikono wakati wa Kutamka *Takbirat Al Ihram* na kuingia Ndani ya Ibada ya Sala hua ni Sunna na kumehimizwa zaid, basi kishariah hua ni bora kuwahi mwanzoni mwa Sala ya Jamaa ili kuipata *Takbir Al Ihram na Raf Al Yadayn* ya Imam na kuna Hadith isemayo kua:

Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaesali Sala zote za Jamaa kwa Ikhlasi kwa mda wa siku 40 mfululizo, huku akiwa ni mwenye kuiwahi Takbir Al Ihram basi ataepushwa na mambo mawili ambayo ni Adhabu ya Moto na Unafiq.**'

Na ingawa kwa Mtizamo wa Imam Al Tirmidhii kuhusiana na Hadith hii kua ni Dhaif Lakini hata hivyo hii ni Hadith inayotuoneshaUmuhimu wa Kuiwahi Takbir Al Ihram ya Imam iwe katika Sala za kawaida au Sala ya Ijumaa na hivyo kutubainishia umuhimu wa Kuwahi mapema katika Safu za mbele Msikitini ili kutochelewa na kisha kisha kukimbilia mbele huku huku ukiwakiuka watu mabega au kujichomeka baina ya watu katika Safu hadi ikafikia hali ya kua Watu mnasali Mabega juu kama mnaumwa na maradhi ya Kukosa Pumzi kwa kubanana.

Na hapo hapo kuwapelekea Maamuma wenzako kusali wakiwa Nyuso zao zimelekea Kibla Halali katika Bayt Al Haram Makkah lakini Mikono na vifua vyao vimeelekea katika Kibla Kilichobatilishwa cha Bayt Al Maqdis Jerusalem. Jambo ambalo ni lenye kukirihisha pale tunapozungumzia kuhusiana na Nguzo ya Tatu ya Sala ambayo ni Kisimamo kama tutakavyofafanua hapo baadae Inshaa Allah.

Na tunakumbushana juu ya hili kosa la kuchelewa Msikitini na kisha kukimbilia katika Safu za Mbele wakati watu wameshakaa au wameshasimama kaa ajili ya kusali, ni kosa ambalo linafanywa na watu wengi sana, labda kwa kutojua au kwa kuajiona tu, kua Mtu kuamia Mimi lazima nisali Safu ya mbele: **'Hivyo hebu mtu huyu na ajiulize kua yeye ndie nani? Na kwanini lazima asali safu ya mbele hata kama itakua amechelewa na hivyo kupelekea kuwavunjia Maamuma wenzake nguzo zao za Sala na hapo hapo kuwakera pia.**'

Hivi jee Waislam hatujui kua hata *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndie Imam Bora zaid na katika Uhai wake alichelewa Msikitini akamkuta Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* anataka kusalisha na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumuondoa Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kwenye Kibla na badala yake *Rasul Allah Sallahu Alayhi waSalam* akawa Maamuma kama Maamuma wengine?

Na si hivyo tu kwani anasema pia Imam Ahmad Ibn Hanbal kua:'**Al Mughira Ibn *Shu'bah Radhi Allahu Anhu* amesema kua: Kuna sifa Mbili ambazo mimi siwezi kumuuliza mtu yeyote yule kuhusiana nazo kwa sababu nimeziona kwa macho yangu zikitekelezwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mbele ya Macho yangu.**'

'Ambazo ni kua Imam kusali Nyuma ya mmoja kati ya Watu ambao ni wafuasi wakeNa nimemuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisali Nyuma ya Abd Rahman Ibn Awf katika Sala ya Alfajir baada ya kuiwahi Rakaa moja.

Na jambo la pili ni kua Nimemuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akipangusa katika Soksi zake katika wakati wa kutia Udhu'*(Musnad Imam Ahmad)*

Hivyo basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae ndie kiumbe pekee aliewasalisha Mitume wote wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ndie.Kiumbe anaestahiki kua Imam kwa viumbe wote, basi hakukimbilia mbele katika Kusali au kusalisha pale alipokua amechelewa kuwasili Msikitini kutokana na dharura mbali ya kua alikua anakaa nyumba ya jirani na Msikiti.

Bali alisali pale pale alipofikia na kuikuta nafasi, hivyo inakuaje leo hii watu wanachelewa halafu wanakimbilia mbele na kuudhi wenzao, kwa kusababisha Safu kubanana hadi kuondoleana Khushuu na kuvunjiana Nguzo zao za Sala?

‘**Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anatoa Khutba ya Sala ya Ijumaa na mara akaingia Sahaba ambae akasogea moja kwa moja hadi karibu ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kuwakiuka watu mabega yao.**

Ambapo baada ya Sala basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Sahaba wake huyo kwa kusema: Hivi kwanini wewe hukusali pamoja nasi Sala ya Ijumaa?.

Hivyo yule Sahaba akasema: ‘Ya Rasul Allah, Hakika mimi nilikua nataka kukaa hapa karibu yako.’

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kumwambia mtu huyo kua: ‘Mimi nimuekuona wewe ukiwakiuka Watu mabega na kuwaudhi, unatakiwa ujue kua Mtu anapomuudhi Muumini basi ha ananiudhi na mimi pia, na anaponiudhi mimi hua anamuudhi na *Allah Subhanah wa Ta’ala* pia.’’

Hivyo ewe Muislam mwenzangu, kama ikiwa Sahaba huyu alikua na sababu tosha ya kutaka kumkaribia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutokana na mapenzi yake na hivyo akawakiuka Waislam wenzake waliokaa kitako kabla yake Msikitini basi aliulizwa: ‘Kwa nini hukusali Sala ya Ijumaa pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake?’ wakati yeye mwenyewe alikua anajihesabu kua Amesali Sala ya Ijumaa pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuuliza Mtu huyo kwa sababu ya kua alikua akijua kua mtu huyo hajui juu ya hayo, na ndio maana akaamua kumbainishia kua Kukiuka Watu Mabega waliokaa kitako Msikitini hua kunapelekea kubatilisha Ibada ya mtu huyo anaekiuka na hivyo hua ni mwenye kuhesabiwa kua ni mwenye kibr na kufanya mchezo badala yake.

Hivyo Ewe Muislam Jitahidi kutofanya yale aliyoyakataza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*hususan pale inapokua lengo lako ni Kutekeleza Wajibu wako wa Ibada ya Kumubudu Mola wako kupitia katika maamrisho na maelekezo ya Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kwani utajikosesha Malipo ya Ibada hio uliyoikusudia na kuhesabiwa kua ni miongoni mwa waliotajwa kua na sifa ya kukadhibisha Dini na kupata dhambi badala yake kutokana na kujumuishwa kwenye ile aya isemayo:

﴿فَوَيۡلٞ لِّلۡمُصَلِّينَ ۝ ٱلَّذِينَ هُمۡ عَن صَلَاتِهِمۡ سَاهُونَ﴾

Fawaylun lilmu<u>s</u>alleena; Alla<u>dh</u>eena hum AAan <u>s</u>al<u>a</u>tihim s<u>a</u>hoona; *(Surat Al Maun 107:4-5)*

Tafsir: ***Na Kisha Ole Wao wale Wenye Kusali. Wale Ambao juu ya Sala zao ni Sahuuna (Wanadharau nazo).***

Na kama unakimbilia kujipachika mbele hata kama umechelewa kwa sababu ya kujiona kua wewe Imam, au mtu mkubwa, unaehishimika katika Jamii na hivyo watu watakuchukuliaje kama wakikuona unasali nyuma Msikitini basi fahamu kua Ibada ya Sala yako hio hua si yenye kua na ikhlasi ndani yake bali ni Ibada yenye Riyah ndani yake, kwa sababu unawajali zaiid viumbe wenzako kwenye Ibada kuliko unavyotakiwa kumjali Mola wako.

Hivyo kila mmoja wetu anatakiwa ajue kua haifai pale unapochelewa Msikitini kisha ukawapangua pangua watu kukimbilia mbele kujipachika ati kwa sababu uwahi Safu ya mbele, kwani katika hali kama hio basi hata kama utaipata safu ya mbele basi hutopata Malipo ya Sala yako kutokana na maudhi yako kwa Waislam wenzako katika wakati wa Ibada na utakua Hujasali bali utapata dhambi za kufanya mazoezi ya viungo Msikitini.

3-AL QIYYAM

❖❖❖❖

QIYYAM - yaani Kisimamo ambacho pia hua kinaenda sambamba na Takbirat Al Ihram, isipokua kwa wale wenye dharura inayokubalika kisharia kama tulivyoona hapo kabla.

Kwawenye Dharura basi wao huwabidi kufanya vile watakavyoweza kulingana na hali zao, yaani kama mtu anaumwa basi na hawezi kusimama basi hatohitajika kusimama bali atakaa kitako, na kama hawezi basi atalala kwa ubavu mmoja wa kulia,na kama hawezi basi kwa ubavu wa kushoto, na kama hatoweza hivyo pia basi atalalia mgongo n.k.Muhimu ni kua katika wakati wa *Takbirat Al Ihram na Raf Al Yadayn* basi Mtu awe ameelekea Kibla, na kama hawezi kunyanyua mikono basi ataashiria tu.

Kwani amesema Imam Abu Amar Al Namari Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalusi Al Qurtubi Al Maliki kua: '**Kusimama katika Sala hua ni Wajib na hakuepukiki isipokua kwa yule mwenye Dharura ya kutoweza kusimama, na hivyo hivyo kuhusiana na kukaa asieweza humbidi kulala n.k kwani Vitu huepushwa kidharura hadi pale mtu atakapokua hana uwezo zaidi wa kuvitekeleza, na hadi mtu akifikia hali ya kupoteza fahamu basindio huepushwa navyo vyote kiutekelezaji'***(At Tahmid)*

Na amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alimtembelea Mtu aliekua akiumwa**, **Na alipofika akamuona Mtu huyo anasali Juu ya Mto, hivyo** ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akauchukua Mto huo na kuutupia pembenilakini mtu huyo akauchukua tena Mto huo na kutaka kusali tena, hivyo*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akauchukua Mto huo na kuutupa tena na kisha akasema kumwambia Sahaba wake huyo kua: 'Sali Sakafuni kama unaweza, na kama huwezi basi ashiria tu kwa kuifanya Sujudu yako kua ni ya Chini zaidi kuliko Rukuu yako**'*(Imam Al Bazzar, Imam Al Bayhaqi)*

Kwani Neno Sala kwa Lugha ya Kiarabu ambalo ni lenye kutokana na herufi Sad, Lam na Waw hua linamaanisha Kua na Maumivu chini ya kifundo cha chini cha Uti wa Mgongo, Kua na Mgongo usiokua na Kibyongo, yaani Ulionyooka kiasi ya kuonekana kama umepinda kwa ndani zaidi kuliko kutoka nje.Na pia neno Sala humaanisha Ibada ya Sala, Dua au Maombi.

Hivyo kwa upande mwengine basi Sala imeitwa Sala kwa sababu ndani yake Inajumuisha Ibada, Maombi na Dua Zinazofanyaa Huku Mfanyaji Ibada hiyo Akiwa ameunyoosha sawia Mgongo wake katika Hatua za ndani ya Ibada hio.Na moja kati ya hatua hizo zenye kuhitajika Unyooshwaji sawia wa mgongo hua ni katika kusimama kunakojulikana kama Qiyyam.

Ambapo neno Qiyyam hua linamaanisha Kusimama kwa Uimara, kwa Utulivu Kwa Wazi bila Kificho, Kunyayuka na kua na Uhai, Kunyanyuka kwa Heshima,Kunyanyuka na kusimama kupingana dhidi ya Uovu.

Hivyo basi Maneno mawili haya Sala na Qiyyam hua yanaenda sambamba kimaana katika Utekelezaji wa Ibada ya Sala Kwani Muumini wa kweli hua ni mwenye kunyooka katika kisimamo chake na kunyooka katika kusimamia Ibada yake na hivyo hua ni mwenye kusimama dhidi ya upinzani wa adui yake ambae ni Ibilisi na hivyo kuonesha Msimamo wake katika Kumuabudu Mola wake.

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿حَافِظُواْ عَلَى ٱلصَّلَوَاتِ وٱلصَّلَاةِ ٱلْوُسْطَىٰ وَقُومُواْ للَّهِ قَانِتِينَ﴾

Hafi*dh*oo AAala alssalawati waalssalati alwusta waqoomoo lillahi qaniteena*(*Surat Al Baqara 2:238)*

Tafsir: ***Kuweni wenye uhifadhi Juu ya SalaHususan Sala ya Kati kati(Ya Al mda wa Asr) Na simameni Mbele ya Allah Mkiwa katika Utiifu wa hali ya Juu kabisa.***

Naam, bila ya shaka hii ni aya ambao inadhihirisha namna gani Waislam tunatakiwa tuwe pale tunapokua tumesimama Ndani ya Sala mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Ambapo kwanza tunapoiangalia aya hii basi tunaona kua intatuhimiza kuhusiana na kuzihifadhi Sala kwa kuzisali katika Nyakati zake jambo ambalo ni lenye fadhilla kubwa sana kama ilivyosema Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pale alipoulizwa na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema: **'Ya *Rasul Allah* hivi jee ni Jambo gani lenye Fadhila kubwa sana zaidi?'**

Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam akajibu: '**Ni Sala zinazosaliwa Katika Nyakati zake'**

Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*akauliza tena: **'Na Baada ya hilo?'**

Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam akasema: '**Kuwahudumia na kuwajali Wazazi Wawili'**

Na kisha Abd Allah Ibn *Masud Radhi Allahu Anhu* akauliza tena '**Na kisha baada ya hilo?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akajibu: '**Kupigana Jihad kwa ajili ya Allah *Subhanah wa Ta'ala'***

Ambapo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: **'Na kama ningeendelea kumuuliza tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi angeendelea kunijibu'**(*Bukhari na Muslim)*

Na anasema *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin Imam Al Mushaqiqin, Imam Al Mufasirin, Zukhruf Ad Din* Imam Al Ghazali Al Thani Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Ibn Al Husayn Al Taymi Al Bakri Al Tabaristan Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kuhusiana na aya hii kua: '**Katika kutuamrisha kwake Kuzihifadhi Sala basi *Allah Subhanah wa Ta'aala* Ametumia hali ya neno ambaho inatumika kwa ajili ya pande mbili zinazohusika katika jambo husika. Kwa Mfano ukitumia neno *Qaatala*basi hua inamaanisha Kuna pande mbili zinazopigana.'**

‘Kwa maana hio basi neno *Haafadha* linamaanisha kua kitendo hicho cha Kuhifadhi hua kinatekelezwa na pande mbili tofauti. Ambapo upande mmoja ni wa Muislam anaesali.Na upande mwengine ni wa nani?’

Na baada ya kuuliza suali hilo basi Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi anaendelea kutujibu wenyewe kwa kusema: ‘**Hapa hua kuna hali mbili kuhusiana na upande huo wa pili, ambapo jibu la kwanza litakua bila ya shaka kua aliekuwepo upande wa pili ni *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Kwani yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie mwenye kumhifadhi Mja wake aliejitolea kwa ajili ya Kumuabudu yeye katika Sala yake na hivyo kumkinga dhidi ya Mitihani ya Misiba mbalimbali kutokana na kuhifadhi kwake Sala. Hali ya pili ni kua ni Sala ndio inayomhifadhi na kumlinda Mja anaezisali kutokana na si chini ya mambo matatu Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

﴿ ٱتْلُ مَا أُوْحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَابِ وَأَقِمِ ٱلصَّلوٰةَ إِنَّ ٱلصَّلوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنْكَرِ وَلَذِكْرُ ٱللَّهِ أَكْبَرُ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ﴾

Otlu ma oohiya ilayka mina alkitabi waaqimi alssalata inna alssalata tanha AAani alfahsha-i waalmunkari walathikru Allahi akbaru waAllahu yaAAlamu ma tasnaAAoona *(Surat Al Anqabut 29:45*)

*Tafsir: **Soma kile tulichokukshushia (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam)ktika kitabu (Cha Qur’an) na Usimamishe Sala kwani kwa hakika ya Sala ni yenye Kulinda kutokana na Dhambi kubwa na Kila uovu.***

Na akasema pia:

﴿يَآأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ ٱسْتَعِينُواْ بِٱلصَّبْرِ وَٱلصَّلاَةِ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo istaAAeenoo bialssabri waalssalati inna Allaha maAAa alssabireena*(Surat Al Baqara 2:153)*

*Tafsir:**Enyi Mlioamini Tafuteni Msaada kutoka katika Subra na Sala kwani kwa hakika Allah ni mwenye kua pamoja na wenye kusubiri***

Na tatu ni kua Sala ndio itakayokuokoa kutokana na Moto wa Jahannam’*(Mafatih Al Ghayb)*

Hivyo basi kulingana na vithibitisho vya Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi basi tunaona kua maana ya sehemu ya Aya ni kututaarifu kua kama tutazisimamia Sala zetu basi nazo pia zitatusimamiana kutuepusha na Maovu na Kutuongezea Subra na kutuepusha na Moto.

Na akasema Al Aalamaa Mula Ali Al Qari Al Hanafi kua:**‘Kua Katika Hali yako ya Kimaumbile Katika Wakati wa Kusali kwa kuikubalisha Sala yako mbeleya Mola wako kwa kufanya Mema na Kuachana na Mabaya kwa kusimamia Masharti ya Sala kama kuuhudhurisha Moyo wako, Kusimamia wakati wake, kuislali katika sehemu bora zaidi, kusimamia ipasavyo mambo yasiokua na uzito yanayojumuisha Sala yako kama Sujud na hivyo kuweza kupata Imani zaidi ya kukubaliwa Sala yako ndani ya Moyo wako kuliko kutokukubaliwa kwake. Na hivyo kua na**

uhakika kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hatokuvunja Moyo kutokana na Wingi Wake wa Rehma, Ukamilifu wa Qudra zake, Wingi wa Ilm yake kwa ajili ya kuhuisha Matumiani na Usafi wa Ibada ya Sala yako.'

Na amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Kulikua kuna Kijana miongoni mwa watu wa Ansari ambae alikua ni mwenye kusali pamoja na *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* na hapo hapo alikua ni mtu ambae si mwenye kuachana na madhambi ya kila aina, na hivyo jambo hili likafikishwa mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo nae akasema: 'Bila yaShaka mwishowe Sala itamuepusha na madhambi hayo. Na haikuchukua mda mrefu isipokua kijana huyo akawa ni mwenye kutubu na kua muongofu, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Jee sikukuambieni mimi?'''**

Hivyo Aya hii nimeitumia kwa ajili ya Uthibitisho wa Nguzo ya Qiyam yaani Kusimamo katika Sala, jambo la pili ni Salat Al Wusta na kisha la Tatu ndio Qiyam, hivyo tuangalie kuhusiana na Salat Al Wusta ambapo tunaona kua kuhusiana na Ufafanuzi wa Neno hili basi Wanazuoni wametofautiana Juu yake, kwani kuna wasemao kua:

Salat Al Wusta ni Sala ya Kati na kati yaani Saa ya Al Asr.
Na kuna wasemao kua Ni Sala zote kwa pamoja.
Na kuna wasemao kua ni Kila Sala ya Kila Siku katika Wakati wake Katikati yake yaani isicheleweshwe wala isisaliwe kabla.
Na kuna Wasemao kua ni Salat Al Jumaa.
Kuna wasemao kua ni Salat Al Idd.
Na kuna wasemao kua ni Salat Al Fajr.

Kwani Anasema Ataa Al Utaradi kua: '**Siku Mimi nisali Sala ya Al Fajir pamoja na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* na hivyo akasalisha na akasoma Qunut ndani yake na baada ya Salam basi akatugeukia na akasema: Hii ndio Salat Al Wusta.'***(Muwatta Imam Malik)*

Ambapo Imam Abu Aliyah ameelezea Tukio hili la Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na kusema kua ilikuaNi Katika Msikiti wa Mji wa Basra nchini Iraq.Ambapo Mtizamo huu ni mtizamo pia wa Abd Allah Ibn Umar, Abu Ummamah na Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhum.*

Na pia ndio mtizamo wa Maimam kama kina Abu Aliyyah, Ubayd Ibn Umay, Ataa Ibn Abi Rabah, Mujahid, Ikrimah na Imam Rabi Ibn Anas.

Na ndio Mtizamo wa Mujaddid Ad Din Mujtahid Imam, Imam Muhammad Idris Al Shafii.Kwani wao wanasema kua: **Sala ya Al Fajir imeitwa Salat Al Wusta kwa sababu ni SalaAmbayo ipo baina ya Salat Al Isha na baina ya Salat Adh Dhuhur, ambazo zote mbili ni Sala zenye Rakaa 4 zinazofupishwa katika Rakaa mbili kwa mtu aliekua Safarini, na huku Sala ya Al Fajr haifupishwi**. **Na kwa sababu Sala ya Al Fajir ni yenye kufuata baada ya Sala Mbili za Sauti yaani Maghrib na Ishaa na ipo kabla ya Sala mbili zisizokua za Sauti yaani Adhuhuri na Al Asr.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ali At Tirmidhii, Imam Abu Muhammad Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Baghawi na Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Al Mawardi ambao wote ni Wafuasi wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii basi wanasema kua: '**Wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Masahaba na wa Tabiiina basi wanasema kua Salat Al Wusta ni Salat Al Asr'**

Kwani katika kuthibitisha kua Salat Al Wusta ni Salat Al Asr basi Al Imam Qadhi Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Al Mawardi Al Shafii ameandika kitabu kizima kiitwacho Tuhfatu Al Ahwadhi ambacho ndani yake mna mitizamo Takriban 40.

Ambapo huo wa kua Salat Al Wusta ni Salat Al Asr pia ni Mtizamo wa Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Said Ibn Jubayr Imam Muhammad Ibn Sirrin, Imam Qatadah Al Sadusi, Imam Ad Dahak Imam Hasan Al Basr,Ibn Al Mundhir Imam Ibn Abd Al Barr Al Maliki, Imam Ibn Attiyah, Imam Abu Hanifa.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua**: 'Asiesali Sala ya Al Asr basi Amali zake zote hua ni bure'***(Sahih Bukhari)*

Na katika vithibitisho alivyotoa Al Qadhi Imam Abu Muhammad Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Baghawi na Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Al Mawardi Al Shafii basi mna Kauli za mtizamo wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Anbas *Radhi Allahu Anhu,*Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,*Abd Allah Ibn *Masud Radhi Allahu Anhu,*Samura Ibn Jundub *Radhi Allahu Anhu,* Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu,* Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu,* Hafsa Bint Umar *Radhi Allahu Anha,* Aisha *Radhi Allahu Anha,* Ummu Habiba *Radhi Allahu Anha,* Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha*. Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*.n.k

Na mtizamo wao unatokana na ile hadith ya Vita vya Handaq ambapo wakati Jeshi la Makafiri likiongozwa na Khalid Ibn Walid kabla ya kusilimu kwake walipowatoa Jasho Waislam kiasi ya kua hawakuweza hata kusali Sala ya Al Asr.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema:**'Allah ayajaze Makaburi yao na Moto, kwani aametuzuia sisi kusali Salat Al Wusta hadi imeingia Magharibi.'**

Na mwishowe *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasali Sala ya Al Asr baada ya Salat Al Maghrib na kabla ya Sala ya Isha.

Ama kwa wale wasemao ni Sala ya Al Asr basi wanasema kua, **'Salat Al Asr imeitwa Salat Al Wusta kwa sababu Sala mbili za Siku hua zinafuatia kabla yake na Sala mbili za Usiku hua zinafuatia baada yake.'**

Ama kuhusiana na wale wasemao kua Salat Al Wusta ni Salat Adh Dhuhr basi wanasema kua : **'Hoja inayokubalika zaidi ni kua imeitwa Salat Al Wusta kwa sababu iko baina ya Sala mbili ambazo moja kati yao ni Sala ya mwanzo kufanywa kua ni ya Fardhi naya pili kati yao ni ya Pili kufanywa kua ni ya Fardhi .'**

Ambapo Imam AbuDaud anasema kua**: *'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Salat Dhuhr katika wakati wa katikati wa Siku na kisha alikua hasali Sala nyengine yeyote ile ambayo ilikua ni yenye kuleta ugumu kwa Masahaba. Na kisha ikashushwa aya isemayo**

﴿حَافِظُواْ عَلَى ٱلصَّلَوَاتِ وٱلصَّلَاةِ ٱلْوُسْطَىٰ وَقُومُواْ لِلَّهِ قَانِتِينَ﴾

Hafi*dh*oo AAala alssalawati waalssalati alwusta waqoomoo lillahi qaniteena*(Surat Al Baqara 2:238)*

Tafsir: ***Kuweni wenye uhifadhi Juu ya Sala Hususan Sala ya Kati kati (Ya Al mda wa Asr) Na simameni Mbele ya Allah Mkiwa katika Utiifu wa hali ya Juu kabisa.***

Ambapo kwa upande wa Zayd Ibn Thabit *Radhi Alahu Anhu*basi anasema kua: **'Salat Al Wusta ni Salat Adh Dhuhr.'**

Na kwa wanaosema kua ni Salat Al Maghribi basi miongoni mwao ni Imam Qubaysah Ibn Abu Dhuayb ambae yeye anasema kua**: 'Salat Al Wusta ni Salat Al Magharibi na hii ni kwa sababu ya Idadi ya Rakaa zake kwani ziko kati kati baina ya Rakaa mbili na Rakaa nne na Rakaa zake hua hazifupishwi katika Sala ya Safari. Na *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* hakuwahi kuirudisha Nyuma wala kuikawilisha. Na Sala hua ni zenye kua na Sauti kabla yake ni kuani za kimya kabla yake.'**

Na amesema *Ummu ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: **'Sala bora mbele *ya Allah Subhanah wa Ta'ala ni Salat Al Maghrib,* kwani haikupunguzwa kwa msafiri wala si kwa mwenyeji, Allah ameanzisha Sala za Siku kabla yake na Sala za Usiku Baada yake, na kama mtu akisali Sala ya Magharibi na kisha akasali Rakaa mbili za Sunna baada yake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamjengea Kasri Peponi, na kwa atakaesali Rakaa nne baada yake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamsamehe Dhambi zake za miaka 20.'**

Na kwa wasemao kua Salat Al Wusta ni Salat Al Isha na hii ni kwa sababu**: 'Iko baina ya Sala mbili ambazo hazifupishwi n inakuja katika wakati wa kulala, na hua inapendekezwa kuichelewesha hivyo hua ni vigumu kuidhibiti.'**

Na kwa wale wasemao kua Salat Al Wusta ni Salat As Subh kwa sababu: **'Iko baina ya mbili za Usiku ambazo ni zenye kusaliwa kwa Sauti na baina ya Sala mbili za Siku ambazo hua ni za Kimya, na kwa sababu ni Sala ambayo inasaliwa wakati watu wakiwa wamelala na kuamka kwake kuisali hua ni kugumu.'**

Na kuna wale wasemao kua Salat Al Wusta ni Salat Al Jumuah na hii ni kwa sababu: **'Watu wanahimizwa kuenda kusikiliza Khutba yake na imefanywa kua ni siku ya Sikukuu'**

Ambapo Imam Muslim ana hadith isemayo kua: **'Amesema Abd Allah kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua: 'Nilikua Nafikiria mimi nimuamrishe mtu asalishe Sala ya Ijumaa na kisha nikachome moto nyumba za wale watu wasiokuja kwenye Salat Al Jumaa.'**

Na kuna wale wasemao kua Salat Al Wusta ni Salat As Subh na Al Asr pia na hii ni kwa sababu: '**Amesema Imam Abu Bakr Al Abhari Kua: '*Amesema Rasul Allah Salallahuym Alayhi wa Salam* kua: Malaika wa Usiku na Mchana hua ni wenye kupishana katika kukusimamieni''**

Na pia kulingana na ile Hadith ya Jabir Ibn Abd *Allah Radhi Allahu Anhu* isemayo kua: **'Sisi tulikua tumekaa na *Rasul Allah Salallahuym Alayhi wa Salam* na mara akangalia Juu mbinguni kwenye Mwezi mpevu mweupe na kusema: 'Kwa hakika mtamuona Mola wenu kama vile mnavyouona Mwezi huu mpevu, kama mkiwa hamtaikosa Sala ya Kabla kuzama kwa Jua (Al Asr) na kabla ya kuchomoza kwa Jua(Al Fajr).''**

Na amesema Umarah Ibn Ruaybah kua: **'Nimemsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua: 'Hatoingia Motoni, Yule ambae aliesali kabla ya Kuchomoza kwa Jua na kabla ya kuzama kwake.''**

Na kuna wasemao kua ni Salat Al Isha na Salat Al Fajr, kwani aliusia Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* Kabla ya kufariki kwake kwa kusema kua: **'Nisikilizeni na Wafikishieni Vizazi vyenuy kua: 'Zilindeni Sala mbili hizi ambazo ni *Salat Al Isha na Salat Al Fajr.* Kwani kama mngekua mnajua vilivyomo ndani yake basi mngekuja kwa ajili ya kuzisali hata kwa kutambaa kwa mikono yenu na magoti yenu.''**

Ambapo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Yeyote yule atakaehudhuria Sala ya Isha katika Jamaa, basi hua ni sawa na aliesali Nusu ya Usiku mzima, na atakaehudhuria katika Sala ya Alfajir katika Jamaa basi hua ni sawa na aliesali Usiku kucha'***(Imam At Tirmidhi na Imam Abu Daud)*

Na ndio maana akasema Imam Said Ibn Musayyib ambae alikua ni Mwanafunzi wa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* anasema kua: '**Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua na wingi wa kutokukubaliana ni ipi ndio Salat Al Wusta kama vile ulivyo wingi wa Nywele zangu.' Na kisha akapitisha mkono wake kwenye nywele zake.**

Ama kuhusiana na:

﴿وَقُومُواْ لِلَّهِ قَانِتِينَ﴾

Waqoomoo lillahi qaniteena*(Surat Al Baqara 2:238)*

Tafsir: ***Na simameni Mbele ya Allah Mkiwa katika Utiifu wa hali ya Juu kabisa****.*

Basi anasemaImam Abu Muhammad Sahl Ibn Abd Allah Al Tustari kua: '**Manemo yasemayo *Waquumuu Lillahi Qanitiina* ni yenye kumaanisha kua, Na Simameni Mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* mkiwa katika Hali ya Utiifu wa hali ya juu Kabisa**. **Na hii ni kwa Sababu Wengi miongoni mwa wenye Kufanya Ibada hua si Watiifu kwani ndani mwao mna Wanafiq, waongo n.k.'**

'Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa: 'Jee ni Ipi ndio Sala Bora?''

Ambapo nae akajibu : 'Ni ile yenye Urefu wa Kisimamo kilichojaa Utiifu.'

Na Zayd Ibn Arqam *Radhi Allahu Anhu* amesema kua: 'Kisimamo kilichojaa Utiifu hua ni Kisimamo Kilichojaa Ukimya ndani yake (isipokua yale yanayotakiwa ndani ya Sala) kwani sisi tulikua tukizungumza maneno mengine pia ndani ya Sala hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala*aliposhusha aya hii, yenye maneno yasemayo *Waquumuu Lillahi Qanitiina(Surat Al Baqarah 2:238) ambapo* baada ya hapo tukawacha kuzungumza ndani ya Sala.'

Na akasema Muhammad Ibn Sawwar kua:**'*Qunut* hua ni Sala ya Witri ambayo ilikua ikiitwa Qunut kwa Sababu ya Dua iliyomo ndani yake ambayo huombwa huku watu wakiwa wamesimama, mbali ya kisomo cha Qur'an, yaani Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kupitia katika Njia ya Dua.'**

Kwani anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Bakr Ibn Farah Al Ansari Al Khazraji Al Andalusi Al Qurtubi kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: Hakika sisi tulikua tukimsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati alipokua akisali**

na yeye alikua akitujibu.Lakini tuliporudi kutoka kwa Najash basi tukamsalimia wakati akiwa anasali lakini hakutujibu.'

Hivyo tukamwambia baada ya kusali: 'Ya Rasul Allah! Hakika sisi tulikua tukikusalimia hapo kabla wakati ukiwa unasali na ulikua unatujibu.'

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Mtu akisali anatakiwa akili yake iwe ndani ya Sala.'

Na amesema Muawwiyah Ibn Abd Al Hakam *Radhi Allahu Anhu* kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesemakua: 'Maneno ya Kauli za Watu hayana sehemu ndaniya ya Sala zetu, kwani Sala hua ni Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* , Kurudia maneno ya Kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta'ala* , Shukrani kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Kisomo cha Qur'an''**

Ambapo anasema Imam Abu Bakr Al Ambari kuhusiana na aya hii kua; '**Wanazuoni Wanakubaliana kua Kusimama kwenye Sala hua ni Lazima kwa kila Mtu Mwenye Afya yake na akaweza kusimama, iwe anasali peke yake au anasali kama Imam au Maamuma.Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Imam amechaguliwa kwa ajili ya kufuatwa, hivyo anapokua amesimama akisali basi na nyinyi simameni.'**

Na Abu Musab *Radhi Allahu Anhu* amesema kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Kama Mtu atasali huku akiwa amekaa Kitako bila ya kua ni mgonjwa basi mtu huyo huwajibika kuirudia Sala yake.'***(Mukhtasar Imam Malik)*

Hivyo kama tulivyosema kuhusiana na Maana ya Sala kua ni kunyoosha mgongo basi inavyotakiwa tunapokua ndani ya Hatua hii ya Kusimama ukiwa umeelekeza kila kiungo cha mwili wako katika upande wa Qibla baada ya kuweka nia na Kungia ndani ya Sala kwa *Takbirat Al Ihram* na *Raf Al Yadayn* basi hua ni Kusimama katika kisimamo cha Sala.

Huku ukiwa umenyoosha Mgongo wako sawasawa, Uso wako ukiwa unaangalia mbele na chini katika sehemu unayosujudia huku ukiwa umewacha nafasi isiyopungua ukubwa wa Nyanda moja baina ya Miguu ya miguu yako katika kusimama kwako.

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: **'Kama Mtu hawezi kusimama kwa Miguu miwili katika wakati wa Kusali na hivyo ikawa amesimama kaa mguu mmoja Basi Sala yake hua Inasihi, lakini kama itakua anayo dharura kinachokubalika kusimama kwake huko mguu mmoja Na hua ni makosa Kusali huku ukiwa Umebana Miguu yote miwili kwa pamoja, bali inapendekezwa kua uiachanishe, na pia ni makosa kusimama huku ukiwa umeweka mguu mmoja mbele na mwingine nyuma, kwani miguu inatakiwa miguu ikae sawasawa huku vidole vya miguu yote vikiwa vimeelekea Qibla.'***(Al Majmuu)*

Kwani wengi miongoni mwa wanaojua siku hizi hua Wanachanua Miguu wakati wanaposali kama kwamba wanataka Kucheza Sumo.Tatizo ni kua katika kujua kwao basi hawajui kua hua haifai kusali na kisimamo cha Kutanua sana miguu na pia haifai kuibana sana miguu kama kwamba uko Jeshini huku ukiwa umeamrishwa kuweka miguu sawa.

Kwani amesema Imam Abu Daud kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisjudu basi alikua akiyatenganisha mapaja yake na wala hakuyagusanisha pamoja.'***(Imam Abu Daud)*

Ambapo hii inamaanisha kua Hakua akitanua sana miguu yake na wala akiibana sana katika wakati wa kisimamo wala wakati wa Sujudu wala wa Attahiyat. Na haya ni Miongoni mwa makosa ambayo kila siku watu wanayafanya ndani ya Sala zao.

Kwani kama tulivyosema kua kuna Watu kwa kujua kwao sana basi Wanatanua Sana miguu, na kuna watu kwa kutojua kwao basi hujipachika kwenye Safu mbali ya kua Safu imejaa, na hakuna nafasi na hivyo kuwasababishia wenzake pamoja na yeye mwenye kusali huku wakiwa wamejibana mabega juu, vifua vimeelekea Bayt Al Maqdis baada ya Makkah na miguu imebanwa pamoja kama wako kwenye gwaride, haya yote hua ni miongoni mwa makosa ndani ya Sala yanayotukosesha fadhila stahiki za Sala zetu.

Kwa sababu anasema Abu Ubaidah kua Siku moja Abd Allah Ibn Masud*Radhi Allahu Anhu* alimuona mtu akiwa anasali huku amebana miguu yake na hivyo akasema: **'Huyu Mtu anafanya Makosa ya Kuenda kinyume na Sunnah, kwani kama angefanya *Murawaha* (angetenganisha miguu yake) basi ingekua bora'***(Sunnan An Nasai)*

Ambapo maana ya Murawaha hua ni kusimama kwa mguu mmoja kwanza na kisha kusimamia kwa mguu mwengine pale mmoja unapokua umechoka na hua pia linamanisha kuacha nafasi baina ya Miguu miwili, hivyo *Rasul Allahs Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* walikua wakifanya Murawaha, yaani hawaku ni wenye kutanua sana miguu kama wachezaji wa Sumo na wala hawakua ni wenye kubana miguu kama Wanajeshi kwenye gwaride, hivyo inatakiwa kusimama kwa kuacha nafasi baina ya miguu, kwa ukubwa usiopungua Nyanda moja.(*Nihayat Al Muhtaj)*

Kwani tunapozungumzia ukamilifu wa Qiyam cha Sala hadi kikafikia katika hali ya *Qanitiin* basi kisimamo hicho lazima kiwe na hali 3 zifuatazo:

'Kusimama huku ukiwa umenyooka Mgongo na kuangalia katika sehemu unayosujudia na Kujisalimisha kikamilifu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kua ni mwenye kumkabidhi *Allah Subhanah wa Ta'ala* Moyo wako na Akili yakoKusimama kwa Utulivu wa hali ya Juu huku ukiwa umeelekea Kibla, yaani bilaYa kutikisika kwa kujikuna jikuna au kugeuka kulia au kushoto.'

Ambapo amesema Mujaddid Ad Din Hujjat Ul Islami Imam Al Shafii Al Thani Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua:**'Maana ya Kisimamo cha Ndani ya Sala kwa muonekano wa nje yake hua ni sawa na Kusimama mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kuhudhurisha Mwili wako na Ufahamu wako kwake. Hivyo unatakiwa uinamisjhe kichwa chako, ambacho ndio kiungo kilichokua Juu kuliko viungo vyote vya kiwiliwili chako.'**

Ambapo maana ya kuinamisha kwako kichwa chako hua ni kuthibitisha kuuinamisha Ufahamu wako kutokana na kila kitu ndani yake na kukisafisha kutokana na Kibri na Kujiona kwako.

Kwani Fahamu kua unakua umesima mbele ya yule ambae Hakuna Mfalme Mkubwa zaid yake Kutokana na kua Watu mnawaogopa Wafalme lakini hamumuogopi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie anaestahiki kuogopwa zaidi ya kitu chengine chochote kile.

Na kutokana na sababu hii basi ndio maana Abu *Bakr Radhi Allahu Anhu* akamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema:

Ya Rasul Allah! Hivi jee tutawezaje sisi kumuogopa na kumuonea Haya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama inavyostahiki?

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Mnatakiwa mumuonee haya na mumuogope *Allah Subhanah wa Ta'ala* zaid ya vile ambavyo mnavyokua mnavyomuonea Haya na kumuogopa yule mwenye Taqwa zaidi yenu miongoni mwenu'.(Ihya Ulum Ad Din)*

Na amesema Imam Ibn Al Qayyim pia kua: '**Mja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*Husimama mbele ya Mola wake mara mbili tu!Ambapo mara ya kwanza ni hapa Duniani katika Kisimamo cha Sala zake. Na mara ya pili hua ni katika wakati wa kukutana nae Akhera Katika siku ya Malipo. Hivyo yeyote yule atakaesimamia kikamilifu kisimamo cha mwanzo basi atakua na wepesi katika kisimamo cha pili. Na yeyote yule anaekidharau kisimamo cha kwanza basi atakua na wakati Mgumu katika kisimamo chake cha pili.**

Ambapo siku moja Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alipokua akisali basi alisoma *Surat Al Mutaffifin*, na alipofikia aya isemayo;

﴿ يَوْمَ يَقُوْمُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعَالَمِيْنَ﴾

Yama Yaquumu Alnnasu lirabbi al aAalamiina*.(Surat Al Mutaffifina 83:6)*

Tafsir: ***Katika Siku ambayo Watasimamishwa watu mbele ya Mola wa Ulimwengu wote.***

Basi Abd Allah Ibn Umar*Radhi Allahu Anhu* aliirudia Ayah hii huku akilia hadi akaanguka na kupoteza fahamu.

Na amesema *Rasul Allah Salallahu Allayhi wa Salam* kua:**'*Allah Subhanah wa Ta'ala* ataendelea Kumgeukia Mja wake, pale wakati Mja wake huyo anapomgeukia kwenye Sala yake, na hivyo Mja huyo akigeuka tu kutoka katika upande wa Mola wake basi na *Allah Subhabah wa Ta'ala* huachana na Mja huyo.'***(Sunnan Abu Daud)*

Na anasema Imam Hasan Al Basr kua: **'Unaposimama kwenye Sala, basi Simama kwa Utiifu na Unyenyekevu kama vile alivyokuamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala*.Na Jihadhari na kua na Dharau, Uvivu na kuangalia huku na kule**. **Jihadhari na kuangalia na kitu chengine wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* yuko mbele yako anatizamana na wewe**. **Jihadhari na kukuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* Pepo yake, bali Muombe hifadhi akuepushe na Moto**. **Usiwe ni mwenye kua na Moyo usiojali na kutokua na muongozo, na wala usiwe na Ulimi usiojua nini unachokisema.'**

Na amesema Imam Zayn Al Aabidin kua: '**Qiyam ni Haki ya Sala yako, hivyo unatakiwa ujue kua Qiyam kinamaanisha Kumkaribia *Allah Subhanah wa Ta'ala***. **Na hivyo wewe hua umesimama mbele yake pale unaposali, na unapolijua hili basi ndio utatamani kusimama basi ndipo utakaposimama ukiwa na hali ya mtu ambae ni Mwenye Kuhitaji msaada mkubwa sana, mwenye kujawa na khofu, mwenye kujawa na matumaini, mwenye Ufukara mkubwa sana**, **mwenye kulia Moyoni na mwenye heshima na unyenyekevu kwa yule aliembele yake Ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala***. **Na hivyo Muonekano wako utakua ni uliojaa utulivu mkubwa sana, kichwa kikiwa kimeinamishwa chini, Viungo vimejaa unyenyekevu, Moyo uliojaa UlainiNa Ulimi wenye kuomba maombi bora kabisa kutoka ndani ya Moyo wako, maombi ambayo ni yenye nia ya kuiokoa shingo**

yako kutokana na Adhabu ya Ufungwa utokanao na Dhambi zako Zitakazopelekea Maangamizo yako kutokana na Matendo maovu yako.'

Subhanah Allah! Naam..hii ni baadhi ya mifano kutoka kwa watu bora waliowahi kuishi baada ya kufariki mbora wa Viumbe yaani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*

Na bila ya shaka kama tutafuata mifano yao, na maneno ya wasia wao wa vipi tunatakiwa tuwe katika Kisimamo cha Sala ambayo ni nguzo katika Nguzo za Sala basi bila ya Shaka tutakua ni watu wenye mabadiliko makubwa Sana katika maisha yetu, kwani tutakua tunafanya Ibada ya Sala ipasavyo na kufanikiwa hapa Duniani na Akhera.Kwani wakati tupo hai basi hatujachelewa kurekebisha kisimamo cha Sala zetu.

Kwani kama hatujajirekebisha basi itakua ni wenye kujiangamiza kwani amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Ameniambia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:Ewe Mtoto wangu, hakikisha kua unaepukana na kukosa Umakini ndani ya Sala Kwani kukosa Umakini wakati ukiwa ndani ya Sala hua ni Angamizo'***(Imam At Tirmidhi)*

Na tunapozungumzia kuhusiana na Qiyam ndani ya Sala basi inatakiwa unaposimama uwe katika hali ya Kutotegemea kitu wala kuegemea kitu kama unao uwezo huo. Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wanasema kua:

Kama ikiwa mtu atasimama huku akiwa ameegemea kitu, katika hali ya kua kama kitu hicho kitaondolewa basi mtu huyo atakua ni mwenye kuanguka chini, basi Sala yake mtu huyo itakua Batili. **Na hii ni kwa sababu ya kua hakusimama mwenyewe peke yake kwa kujitegemea ndani ya Sala yake tendo ambalo ni kuvunja Nguzo ya Sala'**

Lakini kama ikiwa atasimama na kuegemea kitu kiasi ya kua kama kitu hicho kikiondolewa na yeye hatoanguka, basi Sala yake itakua Salama, ila sasa amefanya jambo ambalo ni Makruh. **Na hii ni kwa sababu ya kua hakusimama mwenyewe peke yake kwa kujitegemea ndani ya Sala yake tendo ambalo ni kuvunja Nguzo ya Sala.**

Lakini kama ikiwa atasimama na kuegemea kitu kiasi ya kua kama kitu hicho kikiondolewa na yeye hatoanguka, basi Sala yake itakua Salama, ila sasa amefanya jambo ambalo ni Makruh*(Al Mawsuah Al Fiqhiyah)*

Ambapo tunazungumzia hali hii kwa sababu bado tuko katika kutanabahishana kuhusiana na madhara ya kujichomeka katika Safu za Sala hadi kufikia watu kubanana, na hivyo hutokea lbaadhi ya watu hujikuta wameegemea Nguzo za Msikitini bila kutaka, au kuegemea Rafu za Misahafu n.k.

Na baadhi ya Wakati unakuta Mtu amejibana kiasi ya kua ili asimame sawia basi inabidi awe kama anajilazimisha kuelemea kwa mbele ya Safu, kiasi ya kwamba kama mmoja kati ya watu waliokuwepo pembeni yake atamua kujivuta upande basi mtu huyo alielazimika kujipenyeza na kuegemea wenzake basi atapoteza kisimamo chake na kupepesuka ama kuanguka kabisa, n.k.

Naam..tumetaja Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Malik na Hanbal na baadhi ya Maimam wa Madhhab ya Al Shafii juu ya mtizamo mmoja juu ya Kuegemea kitu katika Kusimama. Hivyo tunaingia kwenye Mitizamo ya Madhhab ya Al Imam Al Shafii kuna *Qawl Al Mutammad* yaani **Kauli inayokubalika zaidi ambayo ni kua Mtu unatakiwa Usimame bila kutegemea Kitu chochote***(Rawdha Talibin)*

Hivyo kuna mtizamo wa kwanza tulioanza nao ambao ni Sambamba na mtizamo wa Madhhab mengine, halafu kuna **Mtizamo mwengine usemao kua mtu unatakiwa usimame mwenyewe bila kutegemea kitu, hivyo ukiegemea Kitu wakati unaweza kusimama mwenyewe basi Sala yako hubatilika iwe kitu hicho kikiondolewa utaanguka ama la***(Ai'ina Thalibin, Asna Al Matalib fi Sharh Rawdh Talibin, Kifayat Al Akhyar)*

Na kwa upande mwengine basi hua haitakiwi Mtu kusali huku akiwa amesimamia mguu mmoja kwa sababu kufanya hivyo hua ni kukosekana kwa Khushuu na unyenyekevu, isipokua pale inapokua kuna dharura ya kufanya hivyo kwa mfano maradhi au hali nyengineyo.

Yaani kwa mfano katika sehemu aliyosimama mtu husika anaesali basi ardhi yake upande mmoja iko juu na upande mwengine hua imeinuka ila sio kama ngazi au kizingiti bali kama mteremko ambao anakabiliana nao mtu kutoka upande wa kulia kwake kuelekea kushoto au kushoto kuelekea kulia ambapo katika hali kama hii basi wakati wa kusali lazima itakua uzito wa mwili hua unazidi kwenye upande wa mguu mmoja uliopo chini kuliko ule ulipo juu, na hivyo mtu unakua huna njia nyengine ya kusali.

Au mfano katika Sala yenye kisomo kirefu basi baadhi ya wakati miguu hua inachoka na hivyo inaruhusika kuhamisha uzito wa mwili kutoka upande mmoja kuuhamishia upande wa pili na hivyo kubadilisha miguu katika kisimamo, huku miguu yote ikiwa chini yaani hairuhusiki kuunyanyua unyayo wa mguu mmoja ukawa juu zaidi ya mwengine.

Na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Sala Bora ni yenye Kisimamo kirefu zaidi'** *(Sahih Muslim)*

Na ndio maana kwa upande wa *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* katika Sala zake basi alikua ni mwenye kusimama Zaidi katika Sala zake kuliko kurukuu au kusujudu na hii ni kwa sababu Kufanya Dhikr ya kusoma Kisomo cha Qur'an hua in bora zaidi kuliko kufanya Dhikr zilizomo ndani ya Rukuu na Sujud. Ambapo hata hivyo baina ya kurukuu na kusujudu basi kusujudu hua kuna Daraja zaid kuliko kurukuu, na hii nikutokana na ile hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambayo amesema ndani yake kua: **'Mja hua karibu zaidi na Mola wake pale anapokua katika Sijda.'***(Sahih Muslim)*

Na kwa kua kusimama na kukaa hua ni sehemu ya vitendo vyo kawaida ya kimaumbile ya Ibn Adam na pia ni sehemu ya vitendo vinavyofanyika katika Ibada basi imebidi kuvitofautisha vitendo hivyo kikawaida na kiibada kwa upande wa Ibada kua ni vyenye kuhitajia kuvifanyia dhikr ndani yake kwa ajili ya kuvisafisha kua ni maalum kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* .NaKurukuu na Kusjudu hua ni kwa ajili ya kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hii ni kwa sababu hua havifanyiki isipokua katika Ibada kwa ajili ya kuabudu.

Hivyo kwa mtu asieweza kusimama kutokana na dharura katika Sala basi hua anaruhusika Kukaa au Kulala kama hawezi kukaa.

ASIEWEZA KUSIMAMA WALA KUKAA KATIKA SALA.

❖❖❖

Hivyo ingawa kusimama sawia, na kutulia bila ya kuegemea kitu chochote pale unapoanza kusali kabla ya kurukuu hua ni Wajib kwani ni nguzo ya Sala, lakini hata hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kutupenda kwake waja wake basi hakutaka kutufanyia ugumu, kwani kwa kua yeye ndie Muumba basi

ni mwenye kujua udhaifu wa maumbile yetu, na kua kuna watakaokua hawawezikusimama kwa sababu wanaumwa, kuna watakaokua wazee, n.k

Na kwa kua Ibada ya Sala hua ni lazima kwa Wanaomuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani ndi njia ya Kumuabudu Muumba na pia ndo njia ya kufutiwa madhamb yao Waumini *basi Allah Subhanah wa Ta'ala* ameamrisha kupitia kwa Mtume wake Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* kua kwa mwenye dharura basi anaruhusika kusali huku akiwa amekaa, na kama hawezi basi asali huku akiwa amelala, n.k kama tulivyoona hapo kabla kwenye Hadith.

Na katika Vitabu vya Fiqh vya Wanazuoni waliotagulia kuna kitu ambacho hua kinajulikana kama Mashaqqah, yaani Mashaka au uzito unaompelekea Mtukutoweza kusimama, kwa mfano labda mtu anaumwa na maradhi ambayo akisimama basi atazidiwa, au anahisi kizunguzungu na hivyo akisimama anahisi kua ataanguka, au akisimama atakua na maumivu ambayo yatamtoa kwenye Sala yake kutokana na kuumwa kwake au Msafiri ambae yumo ndani ya chombo cha usafiri wa baharini na hivyo anaogopa kua akisimama basi anaweza akaangukia Baharini n.k

Ambapo anasema Imam Shams Ad Din Al Ramli juu ya hali hii ya Mashaqqah kua**: 'Mtu anaweza akasali huku akiwa amekaa pale anapokua katika wakati wa hali ya Mashaqqah ambayo yanaweza yakamuondelea hali ya ufaragha wake, n.k'***(Al Taqrirat Al Sadidah)*

Na akasema Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: **'Kama mtu atakua anasali huku amesimama na kisha akawa na khofu ya Mashaqqah au kuongezeka kwa maumivu, au yuko kwenye boti na anaogopa kua ataangukia Baharini, au anahisi kizunguzungu basi hua anaruhusika kusali huku akiwa amekaa kitako'***(Al Majmuu)*

Na Anasema Imam Zakarriyah Al Ansari kua: **'Kama ikiwa Mtu (yuko vitani na amejificha) anataka kusali lakini anaogopa kua kama akisimama basi adui yake atamuona na hivyo kupelekea kudhuriwa au kuuliwa kwake basi Mtu huyo anaruhusika Kusali huku akiwa amekaa au amelala katika sehemua aliyokuwepo.'***(Al Iqna)*

Hivyo kwa upande mwengine basi kama mtu hawezi kusali akiwa katika hali ya kusimama wala kukaa basi atasali katika hali ya Kulalia ubavu wa Kulia huku akiwa ni mwenye kuelekea Kibla(Kama vile anavyolazwa maiti ndani ya Kaburi) ambapo huu hua ni mtizamo wa Madhhab ya Imama Malik, Imam Ahmad Ibn Hanbal na Madhhab ya Imam Al Shafii ambao pia wanasema kua; **'Kama ikiwa mtu hawezi kusali huku akiwa amelala kwa ubavu wa kulia basi na asali huku akiwa amelalia ubavu wa kushoto, na kama hawezi hivyo basi na asali huku akiwa amelalia mgongo huku miguu ikiwa imeeleekea Kibla na kwenye Rukuu na Sijda basi ataashiria kwa kichwa, na ama hawezi kuashiria kwa kichwa basi atatumia macho yake.'**

'Na kwa kua Jukumu la Ibada ya Sala hua halimuondokei Mtu kwa hali yeyote ile, basi kama hawezi kuashiria kwa Macho yake, basi itambidi asali kwa kutumia Ufahamu wake ndani ya akili yake huku akiwa ni mwenye kutumia Ulimi wake kwa ajili ya visomo vya Quran na dhikr vilivyomo ndani ya Sala. Na kama hawezi hata kutumia Ulimi wake basi itambidi kufikiria kuhusiana na visomo hivyo kwenye akili yake paleinapokua akili yake inafanya kazi, hivyo kila mtu anatakiwa atumie uwezo wake katika kutekeleza jukumu lake katika Ibada ya Sala.'

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua; **'Mtu ambae hawezi kusali huku akiwa amesimama wala kukaa basi ataisali Sala yake huku akiwa amelalia mgongo na miguu yake ikiwa imeelekea Kibla na hivyo Rukuu na Sujudu zake zitakua ni za kuashiria kuelekea Kibla. Na kama hali yake itaendelea kua mbaya zaidi basi jukumu la Ibada ya Sala itakua ni lenye kuondolewa juu yake na hivyo itambidi kusali Qadha pale atakapopata afueni.'**

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi**‘Mtu asieweza kusali akiwa amesimama wala kukaa kitako wala kwa kulala basi huondokewa na jukumu la Ibada ya Sala na hatokua na Wajib wa kulipia Qadha baada yake.’**

MTIZAMO WA MACHO KATIKA SALA

❖❖❖

Ama tunapoangalia kuhusiana na mtizamo wa Macho katika wakatikusimama ndani ya Sala kulingana Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua wao wanasema kua: **‘Inavyotakiwa hua ni kuangalia katika sehemu ya kusjudia, na hivyo haitakiwi kuangalia upande mwengine wowote, wala kugeuka au kuchezesha chezesha macho huku na kule, hata kama ikiwa Mtu husika anasali katika sehemu yenye Giza au mtu husika si mwenye kuona yaani ni kipofu’**.*(Tuhfah Al Fuqaha)*

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: **‘Mtu hua anatakiwa kua ni mwenye kuangalia katika upande wa Kibla bila kugeuza geuza kwa mtizamo wake wa Macho, na sio lazima kwa mtu kuangalia katika sehemu unayosujudia, muhimu ni kuangali katika upande wa Kibla hivyo unaweza kumuangalia hata mtu aliekuwepo mbele yako au Imaam wako’**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Al Mawardi Al Shafii na Imam Al Ruyani Al Shafii na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanapendekeza, kua ‘**Mtu anatakiwa awe anaangalia Al Kaabah kama ikiwa Mtu husika anasali ndani ya Masjid Al Haram, na hivyo hua haitakiwi kuangalia katika sehemu ya kusujudia anapokua ndani ya Masjid Al Haram.’**

Tunapoangalia kuhusiana na Mtizamo wa Macho kwa ujumla ndani ya Sala basi tunaona kua kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: **‘Katika wakati wa Kusimama basi inatakiwa mtu kua ni mwenye kuangalia katika sehemu ya kusujudia, na katika wakati wa Kurukuu anatakiwa awe anaangalia katika Vidole vyake vya miguu, na katika wakati wa Kusujudu basianatakiwa kuangalia kwenye ncha ya Pua yake, katika wakati wa kukaa kitako anatakiwa katika mapaja karibu na magoti yake, katika wakati wa kutoa Salam hua anatakiwa aangalie katikaa Bega la kulia anapogeukia upande wa Kulia, na katika Bega la kushoto katika wakati anapogeukia katika upande wa kushoto’***(Imam Zain Al Din Abu Abdullah Muhammad bin Abi Bakr bin Abdul Qadir Al Hanafi Al Razi katika Tuhfa Al Muluk fii Fiqh Madhhab Imam Abu Hanifa)*

‘Kuangalia katika sehemu ya kusujudia hua kunamzuia mtu anaesali iwe Mwanamme au Mwanamke na kumuepusha kutokana na kuvutiwa na kuangalia katika sehemu nyengine zitakazomkosesha utulivu na kumpelekea kumtoa khushuu’*(Maraqi Al Falah)*

‘Hua ni bora kwa Mtuanaesali kua ni mwenye kuagalia katika sehemu ya kusujudia, katika wakati wa kurukuu kuangalia katika miguu yake, katika Sijda yake kuangalia Pua yake na katika kukaa kitako hua ni kuangalia katika mapaja yake’ *(Sharh Al Mukhtasar Al Tahawi -Ahmed bin Ali Abu Bakr Al Razi Al Jassas Al Hanafi)*

Ama Kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: **‘Mtu anaesali anatakiwa Kuangalia Mbele yake, na hivyo kama ikiwa Mtu anaesali atakua anamuangalia Mtoto ambae yuko katika hali ya hatari kama kutumbukia kisimani na kisha akamnadia kumkataza mtoto huyo basi, Sala yake hua haijabatilika, na kama akiwa anawasiwasi na Wanyama wake na akamuona Mbwa mwitu anataka kuwavamia Wanayama wake na akamnadia kumtisha basi**

Sala yake haijabatilika na hivyo anaendelea na Sala yake.'*(Jawaher Al Durar fi hali Aalfaz Al Mukhtasar, Abu Abdullah Shams Al Din Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Khalil Al Tatai Al Maliki)*

Na kwa upande wa Madhhabb ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua:**'Inavyotakiwa hua ni kuangalia katika sehemu ya kusjudia, katika wakati wa kurukuu kuangalia katika miguu yake, katika Sijda yake kuangalia Pua yake na katika kukaa kitako hua ni kuangalia katika mapaja yake', hata kama ikiwa Mtu husika anasali katika sehemu yenye Giza au mtu husika si mwenye kuona yaani ni kipofu, au anasali Salat Al Janaza, hata kama akiwa mbele ya Al Kaabah au nyuma ya *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam'*.**

'Na inaruhusika na hua ni Wajibu kufumba Macho kama ikiwa, kufanya kwake hivyo kutampelekea kutoona kile kilichoharamishwa kukiangalia kama kitatokea mbele yake, hadi yatakapoondka madhara hayo. Na inakirihisha kuangalia Juu Mbinguni.'*(Al Gharar Al Bahiya fi Sharah Al Bahja Al Wardia, Zakaria Ibn Muhammad Ibn Ahmed Ibn Zakaria Al Ansari, Zain Al Din Abu Yahya Al Siniki)*

'Mtu anaesali anatakiwa kudumu katika kuangalia kwenye sehemu ya kusujudia katika Sala zake zote, na hii ndio maana ya Kuangalia katika sehemu ya Kusujudia. Hivyo anatakiwa kuangalia kwenye sehemu ya kusujudia hata kama itakua ni Giza nahii ni kwa sababu kuweka mtizamo wako katika sehemu moja hua ni kujidhibiti zaidi. Na sehemu ya kusujudia ndio sehemu bora na inayohehimika katika Sala kuliko sehemu nyengine zote, isipokua katika wakati wa kutoa shahada ambapo hua ni Sunnah kutoangalia zaidi yancha ya kidole cha Shahada'*(***Fath Al Rahman bi Sharah Zabad, Imam Ibn Raslan, Shihab Al Din Abu Al Abbas Ahmed Ibn Ahmed Ibn Hamza Al Ramli)*

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: '**Mtu anesali anatakiwa kua ni mwenye kuangalia Kibla, au katika sehemu ya kusujudia, na hivyo Mtu husika hua na uhuru wa kuchagua kuangalia wapi kulingana na kule kutakakomplekea kua naKhushuu zaidi ndaniya Moyo wake. Isipokua katika hali mbili zifuatazo:**

1-Anapokua na khofu ya kushambuliwa na Maduai zake, basi anaruhusika kuangalia katika upande waliukuwepo Maadui zake.

2-Pale itakapokua amekaa baina ya Sijda mbili, au katika wakati wa Tahiyyat ambao hua anatakiwa kuangalia kwenye ncha ya kidole chake cha shahada. Hivyo ni bora kwa Mtu anaesali kua ni mwenye kuangalia katika sehemu anayosujudia pale anapokua hayuko katika Kutoa Shahada ndani ya Tahiyyat. Na anapokua anasali katika Masjid Al Haram basi basi anatakiwa kua ni mwenye kuliangalia Al Kaabah iliaaweze pia kupata Malipo yatokanayo na kuliangalia Al Kaabah'*(Tuhfat Al Raakie wa Al Aaajid bi'ahkam Al Masajidi, Imam Abu Bakr bin Zaid Al Jara'i Al Salihi Al Hanbali)*

Hivyo katika Sala hua hairuhisiwi kuangalia pembeni, wala Juu kwani amesema *Ummu Ul Muuminin Aisha Radhi Allahu Anha* kua: '**Mimi nilimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na kuangalia hapa na pale katika wakati ukiwa ndani ya Sala?**

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu: Hiyo hua ni aina ya Wizi ambao Shaytan hua anachukua Sehemu ya Sala ya Anaesali*(Sahih Al Bukhari)*

Kwani anasema Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shibrini Al Khatib Al Shafii kua: '**Hua ni Makruh kugeuza Uso upande wa Kushoto au Kulia kwa sababu kufanya hivyo hua ni**

Wizi unaofanywa na Shaytan kwenye Sala ya Mja anaesali kulingana na Hadith iliyopokelewa na Imam Al Bukhari na kwa sababu kufanya hivyo hua kunamfanya Mtu apoteze umakini na heshima yake. Aidha kama mtu akifanya Makusudi kugeuka kushoto na kulia huku akiwa anajuakuhusiana na Hadith inayokataza, basi hua ni Haram kwake na Sala yake hua inabatilika kama itakua ni mwenye kufanya mchezo.'*(Tuhfat Al Muhtaj)*

Lakini Hata hivyo kama ikiwa kuna dharura itakayompelekea mtu kuangalia upande wake wa Kushoto au Kulia basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Ni Makruh Kugeuza Uso wako upande mwengine katika Sala bila ya Dharura yeyote, lakini kama mtu atageuza uso kwa kutaka kuchunga vitu basi hua si makruh**' *(Al Jawi)*

Hivyo hapa inategemea labda kwa mfano Mama anasali na kisha ana mtoto mdogo ambae yuko karibu yake na analia kwa hali ambayo itakayompelekea kuangalia Upande wa Mtoto wake kuona kuna usalama ama la basi inaruhusika kumtupia jicho, kama kuna hali ya hatari labda n.k na ingawa kutupia macho kwa dharura hua inakubalika katika kua na hali ya Makruh lakini hata hivyo hua haikubaliki kuangalia juu Mbinguni katika wakati wa Sala.

Kwani kwa upande anasema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

مَا بَالُ أَقْوَامٍ يَرْفَعُونَ أَبْصَارَهُمْ إِلَى السَّمَاءِ فِي صَلاَتِهِمْ

Inakuaje hadi baadhi ya Watu wakawa wananyanyua Juu Mbinguni Macho yao katika Wakati wa Kusali?

لَيَنْتَهُنَّ عَنْ ذَلِكَ أَوْ لَتُخْطَفَنَّ أَبْصَارُهُمْ

Kwani Watu wanatakiwa wajidhibiti kutokana na kunyanyua Macho yao Juu katika wakati wa Sala, au la si hivyo basi watapokonywa mtazamo wa kuona wa Macho yao.'*(Sahih Al Bukhari)*

Ambapo maneno ya sehemu ya pili ya hadith hii yametumia *Laam al Amr* (Lamya Amrisho) na ikatumia *Nuun At Tawkiid*(Nuun ya kutilia mkazo) na pia ikatumia Qariina (Kielezo cha Namna) ya hali ya *Tahrim* (Katazo) lake imetumia katazo iliposema Au la sivyo basi Watapokonywa Mtazamo wa kuona wa macho yao.

Na hivyo kumaanisha kua yeyote Yule atakaekua ni mwenye kuangalia Juu au kushoto au kulia badala ya kuangalia Kibla katika wakati wa Sala basi atakua ni wenye kufanya kosa linalostahiki adhabu kubwa ya kupokonywa kitu chenye thamani kubwa kuliko vyote katika uhai wa maisha ya Ibn Adam ambacho ni Kuona kwa macho yake.

Ambapo *Mujaddid Ad Din* Al Hafidh Imam Ibn Hajar Al Asqallani anasema kuhusiana na Hadith hii kua: '**Amesema Imam Ibn Battal kuhusiana na Hadith hii kua Wanazuoni wamekubaliana kua Hua ni Makruh kuangalia Juu katika wakati wa Sala.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Qadhi Al Iyyad Al Andalusi basi amesema kua: '**Hikma ya katazo la Hadith hii ni kua Kuangalia Juu katika wakati wa Sala hua kunaweza kumaanisha kuangalia upande mwengine zaidi ya Kibla.'**

Na akasema Imam Shams Al Haq Al Adhiima Al Aabadi kua: '**Ukweli ni kua kuangalia Juu katika wakati wa Kusali basi kumekatazwa, kutokana na sababu ya Mtizamo wa Macho ya Mtu hauwezi kupokonywa kwa Mtu isipokua kutokana na kuangalia kile kilichokatazwa, ambapo Wanazuoni wa Madhhab ya Al Shafii wamesema kua ni Makruh, lakini kwa upande wa Imam Ibn Hazim Al Andalus basi yeye amekaza kamba zaidi kwani amesema kua kufanya hivyo hua kunabatilisha Sala.***(Aauun Maabud)*

Na amesema pia Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu kua: '***Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Wakati Mja wa Allah anapokua amesimama ndani ya Sala, basi hua hakusimama mbele ya yeyote yule isipokua mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* Na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kusema kumwambia Mja wake huyo kua:Umesimama mbele yangu huku ukimfikiria nani badala yake?Jee kuna mwengine aliekua bora zaidi yangu?Ewe Ibn Adam! Nikaribie karibu kwani mimi ni bora zaid ya huyo unaemfikiria'***(Imam Al Bazar)***

Ambapo hii ni hadith inayotuonesha namna *Allah Subhanah wa Ta'ala* anavyowajali na kuwapenda Waja wake wanaomuabudu, kiasi ya kua anawahimiza kua wasipoteze muelekeo na umakini katika kusimama kwao ndani ya Sala zao.

Tumalizie kuhusiana Mtizamo wa Jicho ndani ya Sala kwa kuangalia hali ya wale wanaosalia njiani kwa mfano katika Sala ya Ijumaa kutokana na kujaa kwa Watu Miskitini na hivyo katika sehemu anayosali mtu akapita Mwanamke wa Wanawake na hivyo mtizamo wa Jicho la Mtu huyo anaesali ukamuangalia Mwanamke huyo, suali ni kua Jee Sala ya Mu huyo itabatilika ama la?

Ambapo anasema Imam Ibn Al Arabi katika Ahkam Al Qur'an kua: **'Inapotokea Mtu anaesali akawa ni mwenye kumuangalia Mwanamke anaepita, bila ya kukusudia basi Sala yake hua haijabatilika hata kama kumuangalia kwake huko kutampelekea kupoteza Khushuu yake ndani ya Sala. Na hata kama atakua ni mwenye kumuangalia kwa mda wa sekunde kadhaa basi hii hua ni mwenye kufanya makosa ya kuangalia kitu kisichohalalishwa kwa Mtizamo wa Macho yake na hivyo akijigundua kua ameangalia kisichoruhusiwa kuangalia basi anatakiwa hapo hapo arudishe Mtizamo wa Macho yake, huku akijitahidi kuitafuta khushuu na unyenyekevu ndani ya Sala yake hio, kwani Khushuu na Unyenyeyevu ndio Msingi wa kukamilisha Sala yake'**

Hii inakua ni kama vile alivyohadithia Aisha *Radhi Allahu Anha*katika Hadith inayosema:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، حَدَّثَنَا سُفْيَانُ بْنُ عُيَيْنَةَ، عَنِ الزُّهْرِيِّ، عَنْ عُرْوَةَ، عَنْ عَائِشَةَ، قَالَتْ صَلَّى رَسُولُ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ فِي خَمِيصَةٍ لَهَا أَعْلاَمٌ فَقَالَ " شَغَلَنِي أَعْلاَمُ هَذِهِ اذْهَبُوا بِهَا إِلَى أَبِي جَهْمٍ وَائْتُونِي بِأَنْبِجَانِيَّتِهِ " .

Amesema Abu Bakr Ibn Abi Shaybah kua amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Al Zuhri kua amesema Urwat kua Aisha *Radhi Allahu Anha* amesema: '*Rasul Allaaah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali kwenye *Khamisaa* (Msala uliotengenezwa kwa Manyoya ya Ngozi ya Mbuzi au Sufi wenye michoro michoro) na hivyo katika Sala yake hio akawa ni mwenye kuangalia Michoro yake hio. Na baada ya Sala akasema: 'Iondoe Khamisa hii mpelekee Abu Jahm na kisha niletee *Inbijaniyah* (Msala wa Sufi usiokua na michoro) kwani *Khamisaa* hii imeniondolea Khushuu yangu ndani ya Sala.''*(Imam Al Bukhari)*

ISTAW – KUGUSANISHA VIDOLE VYA MIGUU NI SUNNA AMA LA?

❖❖❖

Kila mmoja wetu ni mwenye Kuwahi kusikia maneno yafuatayo:

سووا صفوكم فانشويت الصفوف من تمام الصلاة

Sawwuu Sufuufakum Fainna taswiyat Alsfawf Min Tamaam al Salat.

Yaani:**'Wekeni Sawa Safu zenu, kwani kwa hakika Kunyoosha Safu ni sehemu ya Ukamilishaji wa Sala.'**

Ambapo haya ni Maneno ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* Katika Hadith akieleza kwa kusema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiwaambia hivyo Masahaba, Mara baada ya kukimiwa Sala na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anataka watu Wanyooshe Safu katika Qiyam cha Sala zao kabla ya kuwasalisha.

Kwa Hivyo hii ni sehemu ya Sunna kwa Kila Imam kufanya hivyo pale anapotaka Kusalisha na ndio maana hua Tunasikia Maimam wakisema hivyo.

Na kuna Hadith kadhaa ambazo zimezungumzia Juu ya Jambo hili ambapo miongoni mwake kuna zilizotumia maneno kama:

1-Istawwuu(استووا) **Nyoosheni Sala Zenu.** *(Sahih Muslim)*

2-Tarasuut (تراصوت)**Jazeni.** *(Sahih Bukhari)*

3-Sawwuu Sufuufakum(سووا صفوففكم) **Nyoosheni Safu Zenu.** *(Bukhari na Muslim)*

4-IaAtadiluu (اعتدلل) **Simameni Sawa.** *(Imam Abu Daud)*

5-Sudduu al Khalal (سدوا الخلل) **-Zibeni Mapengo (Nafasi zilizowazi). (***Imam Ahmad)*

6-Haadhuu bayna al Manakib (حاذوا بين المناكب)**-Kaeni Sawa baina ya Mabega Yenu.** *(Imam Abu Daud)*

7- Suduu Al Furaj(سدو ا الفرج) **- Unganisheni Mapengo(Nafasi zilizowazi).** *(Imam Ibn Hibban)*

Hivyo basi unaweza ukasikia Imam ametumia moja kati ya meneno haya kabla ya kuingia kwenye Sala na hii ni kulingana na Hadith gani ambayo yeye ameitumia katika kutekeleza Sunnah hii.

Kwani mbali ya Hadith tuliyoanza nayo lakini pia kuna Hadith ya : '**Abu Masud *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua:**

كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَمْسَحُ مَنَاكِبَنَا فِي الصَّلَاةِ، وَيَقُولُ: اسْتَوُوا، وَلَا تَخْتَلِفُوا، فَتَخْتَلِفَ قُلُوبُكُمْ

Rasul Allah Salalalahu Alayhi wa Salam*: Alikua akitushika Mabega wakati tunataka Kusali huku akisema: Wekeni Sawa Safu na msitofautiane kwani Nyoyo zenu zitatofautiana'(Muslim)*

Kuna Hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambayo anasema kua*: '**Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam amesema kua:***

سَوُّوا صُفُوفَكُمْ فَإِنَّ تَسْوِيَةَ الصَّفِّ مِنْ تَمَامِ الصَّلَاةِ

Wekeni sawa Safu zenu kwani Kuweka sawa Safu hua nisehemu ya Ukamilifu wa Sala.'*(Sahih Muslim)*

Kuna Hadith ya Nuuman Ibn Baysir *Radhi Allahu Anhu* isemayo: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akituambia kabla ya kusali kua:**

لَتُسَوُّنَّ صُفُوفَكُمْ، أَوْ لَيُخَالِفَنَّ اللَّهُ بَيْنَ وُجُوهِكُمْ

Nyoosheni Safu zenu au Allah Atazitofautisha Nyuso zenu*(Sahih Bukhari)*

Kuna Hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* isemayo: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akituambia kua:**

وَلَا تَذَرُوا فُرُجَاتٍ لِلشَّيْطَانِ وَمَنْ وَصَلَ صَفًّا وَصَلَهُ اللَّهُ، وَمَنْ قَطَعَ صَفًّا قَطَعَهُ اللَّهُ

Msiwache mapengo (Nafasi katika Safu) kwa ajili ya Shaytan, Kwani kama ikiwa mtu ataziba Safu basi na *Allah Subhanah wa Ta'Ala* atamuunganisha nae(Atakua Karibu nae) Mtu huyo na atakaekata Sala basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamtenga Mtu huyo'*(Sunnan Abu Daud)*

Na pia Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alisema pia kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema:**

أَقِيمُوا الصُّفُوفَ وَحَاذُوا بَيْنَ الْمَنَاكِبِ وَسُدُّوا الْخَلَلَ

Simamieni Safu zenu, Simameni Bega kwa bega na zibeni mapengo.*(Sunnan Abu Daud)*

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hizi kua: '**Hizi ni Hadith ambazo zinahimiza kuweka Sawa Safu katika wakati wa Kusali.**

Na pia ni hadith znazodhihiriaha kua Inaruhusika kuzungumza katika wakati wa kipindi cha baina ya Iqamah na Sala kuhusiana na mambo yanayofaa'*(Al Minhaj)*

Hivyo baada ya kuangalia baadhi ya mifano ya Hadith zinazohimiza kuweka sawa Safu za Sala kama alivyokua akifanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Basi tunaona kua maana ya Amrisho hili la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* inasimamia kwenye Misingi ifuatayo ambayo ni kama alivyosema Mwanazuoni wa Mahiri Sana wa Ilm ya Fiqh na Hadith Madhhab ya Imam Al Shafii mwenye Asili ya Kikurdi aitwae *Al Hafidh Al Kabir Al Mutqin Al Muhariri* Imam Zayn Ad Din Abd Rahman Al Iraqi Al Shafii ambae ndie mwalimu wake *Mujaddid Ad Din* Imam Ibn Hajar Al Asqallani kua:

Malengo ya Kuweka sawa Safu katika Sala hua ni:

1-Kupata Msimamo na Utulivu wa Kituo wa Nje ya Mwili kama inavyowekwa ndani ya Moyo.

2-Kujilinda kutokana na Vishawishi vya Shaytan vinavompelekea mtu kuiharibu Sala yake kwa kua na Shaka ndani yake.

3-Kupendezesha Muoanekano wa Mazingira ya Ibada ya Sala na Wanaoitekeleza Ibada hio.

4-Kuwezesha Maamuma wengi zaidi kujumuika kwenye Sala ya Jamaa, kwani ikiwa kuna Maamuma wengi na Safu zimeacha mapengo basi Safu hazitonyooka.

5-Kuwasaidia Maamuma wasipoteze Umakini ndani ya Sala. *(Tarh Al Tathrib fi Sharh Al Taqrib - Al Hafidh Zayn Ad Din Al Iraqi)*

Kwani Wanasema Masahaba *Radhi Allahu Anhum* kuhusiana na amrisho hilo kua:**‘Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alikua ni mwenye kuwachagua Watu maalum kwa ajili ya kusimamia Unyooshwaji wa Safu za Sala, kwani alikua haingii ndani ya Sala kwa kuanza na *Takbirat Al Ihram* hadi ajiridhishe kwa kutaarifiwa na watu aliowachagua kuangalia Usawa wa Safu kua Safu zimenyooka kama inavyosema Hadithifuatayo:**

أَنَّهُ كَانَ يُوَكِّلُ رِجَالًا بِإِقَامَةِ الصُّفُوفِ فَلَا يُكَبِّرُ حَتَّى يُخْبَرَ أَنَّ الصُّفُوفَ قَدْ اسْتَوَتْ

Hakika yeye alikua aemchagua Vijana kwa ajili ya kusimamia Safu na kisha alikua Hafungi Sala hadi atakapo habarishwa kua Safu zimekaa sawa.

Na akasema pia Suwad Ibn Al Ghaflah kua:

كَانَ بِلَالٌ يَضْرِبُ أَقْدَامَنَا فِي الصَّلَاةِ وَيُسَوِّي مَنَاكِبَنَا

‘Bilal Ibn Rabbah *Radhi Allahu Anhu* alikua akiipiga Miguu yetu kabla ya kuanza kwa Sala na pia kutunyoosha Mabega yetu.’

Ambapo kwa upande wa Baraa Ibn Adhib *Radhi Allahu Anhu* amesema kua:**‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiikagua Safu mwanzo hadi mwisho kwa kutugusa vifua vyetu na mabega yetu na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema kua: *Kwa Hakika Allah Subhanah wa Ta'ala na* Malaika wake wanatuma Salam kwa watu waliowahi Safu ya kwanza.’**

Na tunapozungumzia kuhusiana na Salam inapotoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni Rehma na inapotoka kwa Malaika basi hua ni Dua ya kuombewa anaepewa Salam aongezewe Rehma na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na anasema Nuuman Ibn Bashir *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa*** **Salam alikua akiamrisha kuweka sawa Safu. Ambapo siku moja alitoka nje ya Nyumba yake (kuingia Msikitini) na akamuona Mtu amekaa kwenye Safu huku Kifua chake kikiwa kimetokeza nje ya Safu.*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Nyoosheni Safu kwani vyenginevyo basi Allah atasababisha mgongano kutoka kwenye Nyuso zenu.'***(Imam At Tirmidhii)***

Na akasema Malik Ibn Amir Al Ansari kua: **'Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* alikua akisema kwenye Khutba zake kua:Nyoosheni Safu zenu vizuri na jipangeni kulingana na usawa wa Mabega yenu.'***(Muwata Imam Malik)***

Na amesema pia Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:**'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituambia kua: Unganisheni Safu zenu karibianeni kujipanga kwa kulingana na usawa wa shingo.'***(Imam An Nasai)***

Hivyo Kuweka Safu Sawa na kutoacha mapengo katika Safu katika wakati wa Kusali Sala ya Jamaa hua ni Wajibu ili upatikane ukamilifu wa Sala.Yaani haitakiwi ionekane kua Mmoja kachomoza zaidi mbele au katokeza nyuma ya wengine, hivyo ndivyo inavyotakiwa ziwe Safu za Sala, Watu wazima mbele, Wenye kukalia Viti Pembeni na Watoto Nyuma, na Wanawake nyuma kabisa.

Na ingawa hadith za Kuweka Safu sawa ziko nyingi, lakini hakuna hata hadith moja iliyosema kua:'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alisema kuaTanueni Miguu yenu na Gusanisheni vidole vyenu vya miguu'**, Yaani katika vitu Ambavyo *RasulAllah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuvifuatilia kabisa katika Qiyam cha Sala ni Vidole vya Miguu.

Hivyo*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Makhalifa wake *Radhi Allahu Anhum* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhu* walifuatilia Miguu, Tumbo, Vifua, Mabega na Shingo kwani hivi ndio viungo Muhimu vya Miili ya Ibn Adam kutokana na Kuweza kuonekana kwake kikasoro pale watu Wanaposimama kwenye Safu na hivyo kuonesha kama Safu imekaa Sawa, imepinda au ina pengo, na hivyo ndivyo tunavyotakiwa kufuatilia sisi leo hii, kwa sababu Vidole vimegusana au havikugusana havipewi kipaumbele katika upangaji wa Safu, tofauti na wafuatiliavyo wengi wasiojua leo hii.

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Kuweka sawa Safu na kuziba mapengo au nafasi baina ya Maamuma wanaosali katika Safu, Basi hua Haizungumziwi kuhusiana na Kugusanisha vidole, na hii ni kwa sababu Tukitumia Kipimo cha Vidole vya miguu basi ndio Safu haitokaa sawa kwani kumaumbile kila mtu hua na saizi ya ukubwa wa Mguu tofauti na wa mwenzake kuna wanaovaa size nambari 7, 8, 9 hadi 11 na pia hua kuna utofauti wa vidole, kwani kuna wenye vidole virefu na wenye vidole vifupi n.k

Na Ndio maana Bilal Ibn Rabah *Radhi Allahu Anhu* akawa hawapigi watu vidole vya miguu katika kuwarekebisha katika Safu.Bali alikua anaipiga miguu yaani kwa nyuma..jee unajua kwanini?Kwa sababu Kipimo kinachotumika katika Kuweka mstari sawa kwa mumbile ya Miguu hua ni Kisigino.

Kwa sababu Kisigino ndio kinachoubeba Mwili mzima wa Ibn Adam na Vidole na Nyayo hua ni viungo saidizi tu ili kiwiliwili kiweze kusimama sawia kisianguke, hivyo kisigino cha mmoja kati ya Maamumawaliokua kwenye Safu kikiwa kimetangulia mbele, basi na mtu huyo atakua yuko mbele na hivyo kua tofauti na wenzake katika safu.

Na ndio maana hata katika kupima tofauti baina ya Imam na Maamuma katika Sala ya watu wawili basi hua haiangaliwi kipimo cha vidole bali hua inaangaliwa Kisigino.Yaani Ili Sala iwe ya Jamaa, na Maamuma ikubalike kwa kuridhiwa na Mola wake bila ya kukirihisha Sala yake basi lazima Kisigino cha Maamuma kiwe Nyuma ya Kisigino cha Imam.

Hicho ndio kigezo kinachotumika pale inapokua hakuna nafasi kubwa kiurefu kwa sehemu ya Kusalia, basi inabidi Kisigino cha Imam kiwe mbele, Japo kwa Inchi Moja na cha Maamuma kiwe nyuma japo kwa inchi moja.Kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Zayn Ad Din Al Sunayki Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Masri Al Shafii kua:

'Haiathiri Usahihi wa Sala pale inapokua Nafasi ya Maamuma katika kusimama kua sawa na Nafasi ya Imam. **Kwani tunachokiangalia katika hali kama hii hua ni Kisigino**. **Ambacho ni Kiungo kilichopo nyuma ya Mguu wa Mtu**. **Hivyo hata kama ikiwa Visigino vya Imam na Maamuma viko sawa, lakini kama vidole vya Maamuma viko mbele kuliko vya Imam kwa sababu ya ukubwa wa miguu yake wa Maamuma basi Haitoathirika Sala ya yeyote miongoni mwao.'**

'Na pia Hata kama Kisigino cha Maamuma Kiko mbele lakini Vidole vyake viko nyuma kuliko vya Imam basi Sala ya yeyote miongoni mwao haitoathirika na hii ni kwa sababu Kisigino kinapokua kimetangulia mbele ya mtu basi Mabega ya mtu husika hua pia yametangulia mbele.'*(Asna Matalib)*

Ambapo kwa upande mwingine basi Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari anaendelea kusema kua:**'Hivyo Hukmu ya Sala ya Maamuma ambae anasali huku Kisigino chake ikiwa sawa na kisigino cha Imambasi ni Kua hali hio hua ni Mkaruh***!.'(Fat-h Al Wahhab)*

Kwani kuhimizana kutanua miguu na kugusana vidole katika wakati wa kupanga Safu ni jambo ambalo halina msingi wowote ndani yake wala vithibitisho kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na wasiojua hua wanalisimamia jambo hili kwa nguvu nyingi sana zinazotokana na ari ya Ujinga wao.

Ambapo Jambo la kusikitisha zaidi ni kua hali hii haliko kwa upande wa Wanaume tu, bali pia lipo kwa Upande wa Wanawake.

Kwani mbali ya kua Wanawake hua wanatakiwa kujistiri na kutojiachia miili yao hususan katika Suali la Ibada ambayo inawahudhurisha mbele ya Mola wao.

Hivyo baada ya kujihifadhi kutojiachia kwa kua wako mbele ya Mola wao, basi na wao pia hua wanaamrishwa naWatanuaji Miguu na Walazimishao Kugusana vidole, kua na Wanawake pia hua Wanatakiwa Wagusane vidole vya miguu na Wanawake wenzao wanapokua kwenye Safu.

Na hivyo kupelekea Wanawake kulazimishwa Kutanua Miguu ili wavifikie vidole vya wenzao katika Sala.

Astaghfir Allah.

Hebu fikiri tu Mwanamme amuone Mwanammke ambae amesimama mbele yake huku akiwa ametanua miguu.Jee kwa kiakili na kiufaham Mwanamme atamchukuliaje Mwanammke husika?Yaani ni Mwanammke Anaejiheshimu na Kujawa na Hisia za Haya?Au Ni mwanamke asiejiheshimu, hana hata haya wala haoni aibu?

Kwani kama hio ni kwa upande wa Kiibn Adam tu basi hali itakuaje kwa upande wa Kusimama mbele ya Mola wake akiwa na hali ya kutanua miguu, wakati tunapozungumzia, kuhusiana na Sala ya Mwanammke basi hua ni tofauti na Sala ya Mwanamme.

Kwani Mwanamke katika Sala yake anatakiwa awe na Haya zaid, ajibane jibane asijitanue wakati wa kusimama, kurukuu wala kusujudu kwake na hii ni kulingana na vithibitisho vya Hadith za Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam..Au hili hagulijui?

Kama watu hawajui basi wanatakiwa wajue kua**: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaona Wanawake wawili wakiwa wanasali, na hivyo akawaambia**: '**Mnaposujudu basi Jifanyeni kua ni wenye na udogo zaid ardhini,kwani Mwanamke hua si kama Mwanamme kuhusiana na Jambo hili.'***(Sunan Al Kubra Imam Al Bayhaqi)*

Na amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Wakati Mwanamke anapokaa Kitako katika Sala basi aweke paja lake moja juu ya paja jengine. Na anaposujudu basi na Tumbo lake ligusane na Mapaja yake ili aweze kujihifadhi zaidi kwa kadri awezavyo,na kwa Hakika *Allah Subhanah wa Taala* akimuangalia basi husema: Enyi Malaika wangu nakutakeni kua Mashahidi kua kwa hakika mimi nimemsamehe dhambi zake'***(Imam Al Bayhaqi)***

Na amesema Wail Ibn Hujr *Radhi Allahu Anhu* kua**: 'Amesema *Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam* kuniambia mimi kua: '**Ewe Wail Ibn Hujr, unaposali basi Nyanyua Mikono yako hadi Masikioni, kwani ni kuhusiana na Mwanamke ndio ananyanyua mikono hadi kifuani.'***(Mujam Al Kabir,Imam At Tabari)*

Ambapo anasema pia Imam Ibn Shaibah kua: '**Aliulizwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Sala ya Mwanamke ambapo nae akasema kua: '**Mwanamke anatakiwa ajibane na kijifanya kuonekana kua na maumbile yenye udogo wa kimwili.'**

Na akasema Imam Abd Razak kua:'**Amesema Ali Ibn Anbi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: Mwanamke akisjudu basi anatakiwa ajifanye mdogo, tumbo lake ligusane na Mapaja yake na agusanishe Mapaja yake.'**

Na amesema *Mujaddid Ad Din Mujtajid*Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: **'Hakuna tofauti ya Vitendo baina ya Sala ya Mwanammke na MwanammeIsipokua anatakiwa Mwili wake ushikamane na mwili wake, Tumbo lake lishikamae na Malaja yake katika Kusjudu katika hali ambayo atakua amefichikana vya kutosha, na anatakiwa awe na hali hii katika Sala yake yote. Na Jilbab lake liwe pana lisishikamane na mwili wake katika wakati wa Kurukuu na kusjudu ili nguo zake zisiainishe Mwili wake na Sauti yake iwe ya Chini, hivyo chochote kikitokea kwenye Sala ya Jamaa basi na apige makofi kumkosoa Imam'***(Al Mukhtasar)***

Mwanammke hatakiwi kujiachia na kujitanua katika Sala bali anatakiwa ajikunyate na abane Miguu na mwili wake wote kwenye Sala, kwani kufanya hivyo ndio hua kuonesha Heshima, Unyenyenyekevu na Haya Mbele ya Mola wake.

Ambapo hua wanaamrisha na kufanya haya wanayoyafanya kwa kutumia maneno ya Sahaba yaliyomo katika hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua: '**Mara moja baada ya Kukimiwa Sala basi alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*:Nyoosheni Safu zenu kwani kwa hakika mimi nnakuoneni kupitia kwa upande wa Mgongoni mwangu.'**

Ambapo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu anhu* anaendelea kusema kua: '**Hivyo tulikua tukiunganisha Mabega yetu na miguu yetu na Mabega na miguu ya mtu aliekua pembeni yetu.'***(Sahih Bukhari)*

Na pia katika Hadith ya Nuuman Ibn Bashr *Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema kua: '**Niliona Mimi kua kila Mtu akiunganisha Manega yake kwenye Mabega ya mwenzake, Magoti kwa Magoti na Kifundo cha Mguu kwa Kifundo cha Mguu wa Mtu wa Karibu yake**.'*(Imam Abu Daud)*

Kwani hizi ni hadith ambazo zinaonesha namna Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walivyokua wakijitajidi Kunyoosha Safu zao za Sala.

Na kwa kua maneno yakiyoongezewa kufafanua kilichotokea yalikua ni ya Masahaba basi maneno hayo hua si uthibitisho kua kuna Maamrisho ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Kuwaambia Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kua watanue Miguu yao au wagusanishe Vidole vya Miguu yao au wagusane miguu yao.

Na ndio maana *Mujaddid Ad Din Al Imam Al Hafidh Al Kabir Shaykh ul Islami Imam Al Aimah Aalam al Aalam* Ahmad Ibn Ali Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii akasema kuhusiana na Hadithi hii kua: '**Maana ya Hadith hii ni kuonesha Umuhimu wa Kunyoosha Safu na kutoacha Nafasi baina ya Watu kwenye Safu.'***(Fat-h Al Barr)*

Ambapo katika kuiainisha kwake Hadith hii basi Mujaddid Ad Din Al Hafidh Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi ameiweka kwenye kichwa cha '**Habari kiitwacho Mubalagha yaani Kuzidisha kitu hadi kikapitiliza zaidi ya hali yake ya kawaida au kuzidisha chumvi.'**

Ambapo mtizamo huu pia ndio mtizamo wa Al Imam Al Allamah Al Hafidh Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhammad Al Qastallani Al Shafii katika kitabu chake cha Irshad Al Sari ambacho kinakimbizana na Fat-'h Al Barr kwa Ubora.Na pia Al Allamah Imam Badr Ad Din Al Aynii amesema hivyo hivyo kuhusiana na Hadith hii katika Umdat Al Qari.

Hivyo kuhusiana na Kusimama katika Safu ya Sala basi kwa Wanaume haitakiwi kuacha Nafasi, haitakiwi kutanua miguu sana wala kuibana sana na wala si lazima mkanyagane au mgusane vidole kwani Muhimu ni kugusana mabega ambayo kutokana nayo basi Kifua kinatakiwa kielekee Kibla na Safu imekaa sawia.

Na kwa Wanawake ndo kabisa haitakiwi kutanua miguu, wala Kugusana vidole vya miguu kwani hadith zimesema yagusane mabega.

Na kama alivyosema Imam Al Asqallani na Imam Al Qastallani kua Kufanya hivyo hua ni kuongeza chumvi. **Na chumvi ikizidi katika kitu basi utamu wake hutoweka na kitu husika hua ni chenye kukirihisha.**

Na hivyo kutojitanua Miguu katika kisimamo na kutogusana Vidole hakumpelekei Mtu kutakiwa kuleta Sijdat Sahw...kwa sababu hua si kupunguza wala kuzidisha kitu dani ya Sala.

KUFUNGA MIKONO

❖❖❖

Bado tupokatika sehemu ya Qiyam cha Sala ambayo ni Nguzo ya Tatu ya Sala.Ambapo ndani yake tunaona kua kuna kitendo cha Kufunga Mikono ambacho hua kinafuatia mara tu baada ya mikono hio kurudi kutoka katika hali ya *Raf Al Yadayn* yaani kunyanyua Mikono katika wakati wa kutamka*Takbirat al Ihram* yaani Allahu Akbar! ya mwanzo kabisa ya kuingilia ndani ya Sala.

Kwani amesema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Sisi Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tumeamrishwa kuharakisha Iftar (kufungua Saumu) zetu, kucheleweshe Imsak – (Kufunga Saumu au kula Daku) zetu na Kufunga mikono yetu kwa kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto katika Sala.'**

Na ingawa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Abu Hanifa.

Lakini Wafuasi wa Madhhab mengine yaliyobakia ya Kiislam hua hawafungi mikono bali hua wanaiachia, na miongoni mwao ni Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik.

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Na kwa Upande wa Imam Malik basi kuna Hadith zisemazo kua Ni vizuri kufunga Mikono katika Sala za Sunnah na ni Bora kuachia Mikono Katika Sala za Fardhi , na hivyo hili ndio jambo ambalo Wafuasi wa Basra wamelipa kipaumbele.**' *(Sharh Sahih Muslim)*

Hivyo hio ni kuhusiana na kuachia mikono kwa upande wa Wafuasi wa Madhhab mengine ya Kiislam wanaoachia Mikono katika kufunga Sala. Kwani amesema pia Imam An Nawawi kua: **'Amesema Imam Al Layth Ibn Saad kua Mtu anaesali na kuachia Mikono basi anaweza kuifunga kama ikiwa Sala ni ndefu'***(Al Majmuu)*

Ambapo hapa inabidi tujuekua Imam Al Layth Ibn Saad alikua ni Imam Mcha Mungu Mkubwa sana wa Misri ambae alikua na Ilm kubwa sana kuliko hata Imam Malik Ibn Anas ambae ni muanzilsiahi wa Madhhab ya Imam Malik. Na Imam Muhammad Idris Al Shafii aliamua kuhamia katika Ardhi ya Misri kutoka Baghdad baada ya kusikiakua katika Ardhi ya Misri kuna Mwanazuoniambae ana Ilmu kubwa sana aitwae Imam Al Layth Ibn Saad.

Lakini hata hivyo wakati Imam Muhamamd Idris Al Shafii alipokua njiani kuelekea Misri basi akapata habari kua Imam Al Layth amefariki Dunia.Na hivyo Imam Al Shafii akaendelea na Safari yake na alipofika katika ardhi ya Misri basi akasoma kwa Wanafunzi wa Imam Al Layth ili apate Ilm ya Imam Al Layth.

Ambapo kwa upande mwengine basi tunaona kua Imam An Nawawi anasema kua: '**Imam Al Awzai amesema kua Mtu hua ana khiari ya kuchagua baina ya kufunga mikono na kuachia katika Sala.**'*(Al Majmuu)*

Na tumeanza na mtizamo huo wa kuachia mikono katika Sala kabla ya kuingia kwenye Vithibitisho vya Hadith za kufunga mikono kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii si kwa sababu ya kutaka kubishana au kukosoa.Bali ni kwa sababu ya kuondoa shaka, na tofauti ambazo baadhi ya Wakati hujitokeza kutokana na baadhi ya watu kujiuliza masuali kwanini hawa wanaachia mikono na sisi hua tunafunga mikono katika Sala.

Hivyo ili tusiulizane wala kudhaniana vibaya miongoni mwetu Waislam basi ni muhimu kwanza kufaham kwanini wao wanaachia mikono na sisi tunafunga mikono. Ambapo anasema Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki kua: '**Na kuweka Mkono mkono wa Kulia juu ya Mkono wa Kushoto, au Kuiwachia hua ni Miongoni mwa Sunna za Salat'**(*Al Kafi fii Fiqh Ahl Madina Al Maliki)*

Na bila ya shaka ukweli ni kua kuna Hadith ambazo zinaunga mkono Kufungua Mikono na kuna zinaunga mkono Kufunga mikono ndani ya Sala, kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alionekana katika Sala zake baadhi ya Wakati amefunga Mikono na baadhi ya Wakati alikua akifungua.

Na ndio maana Wanazuoni wametofautiana juu ya Jambo hili, kulingana na Vithibitisho vya Hadith Husika na hivyo hua hakuna kosa kwa anaefunga na pia hakuna kosa kwa anaefungua Mikono.

Ambapo anasema Imam Az Zaylai kua: '**Abd Allah Ibn Mubarak alikua akinyanyua mikono katika wakati wa kusali na yeye ndie aliekua ni mwenye Ilm, kubwa sana miiongoni mwa watu katika wakati wa Uhai wake, ambapo anasema Abd Allah Ibn Mubarak kua: 'Nilisali mimi pembeni ya**

Nuuman Ibn Thabit(Imam Abu Hanifa) na nikanyanyua mikono yangu, ambapo nae baadae akaniambia kua: 'Hakika mimi nilikua na khofu kua huenda ikawa ulikua unataka kuruka baada ya kukuona ukinyanyua mikono' hivyo nami nikamwambia Nuuman kua: 'Kua sikua nikijaribu kuruka katika mara ya mwanzo nilipokua nikinyanyua mikono basi bila ya shaka na hata katika mara iliyofuatia pia sikua nikijaribu kufanya hivyo''

Ambapo amesema Imam Waki Ibn Jarrah kua: 'Allah amuingize kwenye rehma zake Ibn Mubarak kwani alikua ni mwenye kua na majibu tayari ya hapo kwa hapo''

Nakisa hiki kimenukuliwa na Imam Waki Ibn Jarrah ambae amesema kua: **'Nilisali mimi katika Masjid Kufah, ambap ndaniyake alikuwepo Abu Hanifa aliekua amesimama akisali na pembeni yake alikuwepo Abd Allah In Mubarrak, ambae alikua akinyanyua mikono kila anaporukuu na kila anaponyanyuka kutoka katika rukuu, na baada ya kusali basi Imam Abu Hanifa akasema:**

'Ewe Abu Abd Al Rahman, Nimekuona mimi ukinyanyua mikono yako, kila wakati, Jee ulikua unataka kuruka?'

Abd Allah Ibn Mubarak akasema: 'Ewe Abu Hanifa nilikuonamimi pia wewe ulinyanyua mikono yako wakati ulipokua ukifunga Sala katika *Takbrirat al Ihram,* Jee ulikua unakusudia kuruka?'

Imam Waki' anaendela kusema: 'Hakika mimi sikuwahi kumuona mtu mwenye Ufahamu wenye majibu ya haraka zaidi na ya hapo kwa hapo kama Abd Allah Ibn Mubarak kwa Abu Hanifa.''*(Ta'wīl Mukhtalif Al-Hadīth, al-Tamhīd – ImamIbn Abdul-Barr)*

Ambapo pia tukio kama hili tunaliona kwa upande wa Imam Al Awzai na Imam Sufyan Ath Thawry pale walipokutana katika katika Masjid Al Khaif walipoanza kuhojiana kuhusiana na kunyanyua mikono katika wakati wa Kurukuu na baada yake, na hivyo Imam Al Awzai akasema kua: **'Amesema Al Zuhri kua amesema Salim kua amesema Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akinyanyua mikono katika wakati wa Kurukuu na kunyanyuka kutoka katika Rukuu.''**

Hivyo Imam Sufyan Ath Thawry akasema kua: **'Kulingana na hadithi ya Yazid Ibn Abi Zayd, basi ni kua *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* hakufanya hivyo.'**

Na Imam Al Awzai akauliza kwa kusema: **'Hivi Jee ni nani anaeweza kushindana na Hadith ya Al Zuhri kutokana na Hadith ya Yazid Ibn Abi Zayd? Ambae ni mtuu dhaifu?'**

Hapa muonekano wa uso wa Imam Sufyan Ath Thawry ukawa mwekundu na Imam Al Awzai akasema: **'Inawezekana ikawa wewe hukupena kile nilichokisema mimi?'** na Imam Sufyan Ath Thawry akasema: **'Naam!'**

Imam Al Awzai akasema: **'Kama ni hivyo basi twende pale kwenye pembe za Al Kaabah, na kisha tunyanyue mikono juu tuapizane kuhusiana na ni nani alie sahih miongoni mwetu'** na hapo Imam Sufyan Athawry akabakia kimya.*(Bidāyah al-Nihāyah)*

Hivyo Al Faqih Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Muhamad Ibn Rushd Al Qurtubi Al Maliki Al Andalus anasema kua: '**Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Sehemu ya kuweka**

Mikono, kwani kuna wasemao unaweka hivi Mikono na kuna wasemao unaweka vile Mikono ndani ya Sala.

Ambapo kwa Upande wa Imam Malik basi yeye anasema kua Hua ni Makruh katika wakati wa Sala ya Fardhi kwa mtu kua ni mwenye kufunga mikono, lakini hua inaruhusiwa katika wakati wa Sala ya Sunnah. **Ambapo kwa upande wa Wale wanaofunga Mikono basi huchukulia kitendo hicho kua ni sehemu ya Sunnah za Salah**. **Ambapo wasemao hivi ndio wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Karne za Mwanzoni za Uislam.'**

Na sababu ya Kutofautiana kwao ni kutokana na misingi ya Hadith za Masahaba *Radhi Allahu Anhu* na Tabiina waliowafuatia. **Kwani Uelezwaji wa Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kusali kwake kumeelezewa ndani yake kupitia kwao wao.**

Na kwa upande mmoja basi hakuna sehemu iliyotajajwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliweka Mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto. **Ambapo kwa upande wa pili basi pia kuna uthibitisho wa Kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaamrisha watu wafunge mikono.**

Na kufunga Mikono pia kumeelezewa kua ni sehemu ya Namna alivyokua Akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* katika Sala zake, kwa mfano katika Hadith ya Abu Hamid. **Na hivyo Wanazuoni wamethibitisha kua Kufunga Mikono hua ni kitu kunachohesabiwa kua ni Sunnah katika Hadith zenye kuunga mkono Kufunga mikono, na hivyo Kuna Ulazima wa Kuifuata Sunnah hio**.

Na kuna wanaoona kua bora kufuata Hadith zisizokua na Sunna hioNa hii ni kwa sababu kufunga Mikono hua si sehemu ya Sala bali hua ni sehemu ya Kujiongezea Utulivu ndani ya Sala.'*(Al Muqaddimah Ibn Rushd)*

Na Imam Ibn Qutaybah kua amesema: **'Abu Ahwas kua amesema Samak Ibn Harb kua amesema Qabisah Ibn Hulb kua amesema Baba (*Hulb at Tai Radhi Allahu Anhu)* yake kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akituongoza Sisi kwenye Sala na alikua akiifunga Sala kwa kuukamata Mkono wake wa kushoto kwa Mkono wake wa Kulia. '***(Tuhfat Al Ahwadh Fi Sharh Jamii Tirmidhii)*

Na anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua:**'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuona Mtu akiwa anasali huku akiwa amewrka mkono wake wa kushoto juu ya mkono wa Kulia na hivyo akamsogelea na kuuukamata Mkono wake wa Kulia na kuuweka juu ya Mkono wa Kushoto.'** *(Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo anasema Saad Ibn Sahl kua: '**Watu wameamrishwa kuweka mikono yao ya kulia juu ya mikono ya shoto wanaposali.'**

Ambapo kwa upande wa Wail Ibn Hajr *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Mimi nilisali *na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alifunga mikono kwa kuweka mkono wake wa Kushoto juu ya mkono wa kulia kwenye kifua chake.***'(Imam Ibn Khuzaymah, ImamAt Tirmidhii na Imam Al Bazar)*

Ambapo anasema Imam Abu Daud kua: **'Amesema Jarrir Ad Dabi kua Mimi nilimuona Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akisali huku akiwa amekamata kiganja chake cha mkono wa kushoto kwa mkono wake Wa Kulia ikiwa kwa juu ya Kitovu chake.***'(Sunnan Abu Daud)*

Na katika Musannaf Imam Ibn Abi Shaybah kuna hadith isemayo kua: **'Amesema Wail Ibn Hajar kua: Mimi nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa ameweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto chini ya kitovu chake.** *'(Musanaf Ibn Abi Shaybah)*

Kwa maana hio basi mbali ya kua kuna Hadith zisemazo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali huku akiwa amewachia Mikono lakini pia kuna Hadith ambazo zinazosema kua alifunga Mikono.Ambazo zinaelezea Sehemu 3 tofauti kwani kuna zisemazo kua:

1-Alifunga Mikono Kifuani. *(Imam Ibn Bazar)*

2-Alifunga mikono chini ya Kifua. *(Imam Ibn Khuzaymah)*

3-Alifunga mikono Chini ya Kitovu. *(Imam Ibn Abi Shaybah)*

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi ni kua Mikono hufungwa Chini ya Kitovu kwa Mwanamme na juu ya kifua kwa Mwanammke.

Madhhab ya Imam Malik ni kuachia Mikono lakini kama unataka basi utafunga chini ya Kifua.

Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ni kua Utafunga Juu ya Kitovu yaaniKifuani.

Ambapo anasema Imam Abu Isa Muhammad Ibn Isa As Sulami At Tirmidhii kua: **'Wenye Ilm miongoni mwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Na waliofuatia baada yao na baada yao wanaamini kua Mtu anatakiwa aweke Mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto, ambapo baaadhi yao wanasema kua juu zaidi ya Kitovu na kuna wasemao chini ya Kitovu.'**

Na ingawa kuna utofauti huo kwa upande wa Wanaume kufunga mikono yao lakini kwa Upande wa Wanawake basi Wanazuoni wanakubaliana kua: '**Wanawake wanatakiwa Wafunge mikono tofauti na Wanaume kwani Wanaume hutakiwa mkono wa kulia kukamata mkono wa kushoto, lakini kwa upande wa Wanawake hutakiwa kuiweka tu mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto bila ya kuukamata mkono huo ambapo mikono hio itakua imekaa Kifuani Kwenye Maziwa yao, yaani isiwe chini ya Maziwa wala juu ya Maziwa.Yaani Mikono isiwe imebeba Maziwa na wala isiwe Imeyabinya Kwa Juu na kisha yakatokeza kwa chini.Bali iwe kama iliyoyafunika na kuyahifadhi zaidi maumbile ya Maziwa yao.'**

Najua kua kuna wakataosema kua sijagusia kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kwa Upande wa Wanaume, lakini mbali ya kua Tumeangalia Mtizamo wa Imam Al Tirmidhii ambae ni mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Lakini ukweli ni kua hii ni kwa sababu kwa sababu ya kua kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi nataka tuzamie kidogo katika kufahamishana katika kurasa zinazofuatiahivyo na tuangalie mtizamo wa Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazal al Tusi Al Shafii ambae ni Mujaddid Ad Din na Mujtahid Imam wa Madhhab ya Imam Al Shafii na As-hab Al Wujuh wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambae anasema kua**:** '**Sunnah ya Kufunga Mikono Ndani ya Sala ni kuiweka Chini ya Kifua'***(Al Wasit)*

Na kama tunavyojua kua tunapozungumzia Mtizamo wa Fiqh wa Madhhab husika basi hii hua haimaanishi huo unaozungumziwa hua ndio Mtizamo wa Imam Mkuu wa Madhhab.Kwa Mfano Imam

Mkuu wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni Mujaddid Ad Din, Mujtahid Imam Muhammad Idris Ak Shafii na hivyo yeye hua ana Mitizamo yake inayochukuliwa kua ni Mitizamo ya Imam Mkuu.

Lakini hata hivyo kwa upande wa Kila Madhhab ya Skuli za Fiqh basi mbali ya kua kuna Mtizamo wa Imam Mkuu wa Madhhab lakini pia hua kuna Mitizamo ya Maimam waliochini ya Imam Mkuu ambao wao Darja yao ya Kiilm hua ni ya Hali ya Juu katika Madhhab husika, na darja yao hua hawaipati kwa kujipa wao wenyewe, bali hua wanapewa kutokana na kukubalika kwa ukubwa wa Ilm yao.Na hivyo basi Mitizamo ya Wanazuoni hawa ndani ya Madhhab husika kuhusianana jambo husika hua linaangaliwa na kuchunguzwa ndani ya Madhhab kuonekana kama linakubaliana na Mtizamo wa Imam mkuu wa Madhhab ama la.

Kwani Kiislam vitu vinavyovyopewa kipaumbele katika vyanzo vya Sharia ya hua ni Qur'an kisha Sunna na Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Kisha kinachofuatia hua ni Makubaliano ya Wanazuoni, kwani alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:***'Allah Subhanah wa Ta'ala*** **hatoujaalia Ummah wangu kukubaliana juu ya Maovu.'** *(Imam At Tirmidhii)*

Na ndio maana akasema Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali kua: **'Muislam Atakaepingana na Makubaliano ya Wanazuoni hua ni mwenye kujitoa ndani ya Umma wa Kiislam.'**

Hivyo Muislam ukisikia kua Juu ya jambo fulani wamekubaliana Wanazuoni basi mimi na wewe hua hatutakiwi kupingana nalo, kwani kufanya hivyo hua ni kuenda kinyume na maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na pia maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Surat An Nisaa 4:115 ambayo yanasema kua:

﴿وَمَن يُشَاقِقِ ٱلرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ ٱلْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ ٱلْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ وَسَآءَتْ مَصِيراً﴾

Waman yushaqiqi alrrasoola min baAAdi ma tabayyana lahu alhuda wayattabiAA ghayra sabeeli almu/mineena nuwallihi ma tawalla wanuslihi jahannama wasaat maseeran*(Surat An Nisaa 4:115)*

*Tafsir:**Na atakaemtilia shaka Rasul (AllahSalallahu Alayhi wa Salam), baada ya kubainishiwa njia Sahih, na kisha akafuata njia isiyokua ya Walioamini basi tutamuelekeza katika njia hio na kisha tutamtia Motoni, ambayo ni mafikio mabaya sana.'***

Hivyo basi tunaporudi katika Mitizamo ya Madhhab, basi hua kuna Mtizamo wa Imam Mkuu na Mitizamo ya Maimam Wakubwa Waliokubaliana juu ya jambo husika.Kwa maana hio kama ikiwa Mtizamo wa Imam Mkuu unapingana na Mtizamo wa Makubaliano ya Maimam wengine wa Madhhab husika, basi hapa Mtizamo wa Imam mkuu hua hauna nguvu, kwa sababu Wanazuoni Waliokubaliana juu ya jambo husika ni wengi na hivyo Mtizamo wao ndio hua mtizamo wa Madhhab husika.

Na hapo kabla nilipomtaja Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhamamd Ibn Muhammad Ibn Muhamamd Al Ghazali katika sifa zake basi nilimtaja kwa jina la *As-hab Al Wujuh*.Na hii ni kwa Sababu katika Madhhab ya Imam Al Shafii baada ya Imam Al Shafii mwenyewe basi kuna Wanazuoni wakubwa wanaotisha kwa Ilm ambao ndio hua wanajulikana kama As-hab al Wujuh yaani Watu wanaoupa Muonekano wa Sura Sahih ya Madhhab ya Imam Al Shafii na hivyo hua na Kauli pia na mitizamo yao ikikubaliana basi ndio hua mtizamo wa Madhhab.

Kwani kuna ngazi 5 za daraja la *Mujtahid* kwa mujibu wa Madhhab ya Shafi'i:

1 – ***Mujtahid Mutlaq*** (Mujtahid kabisa), yaani Imam Al Shafi'i, Imam Malik, Imam Abu Hanifah na Imam Ahmad Ibn Hanbal *Rahimahumullahu Ta'ala.*

2 – ***Mujtahid Muntasib*** (mwanasheria mshiriki), kama Imam Ibn Khuzaimah, Imam Ibn Mundhir, Muhammad Ibn Jarir na Imam Muhammad Ibn Nasr,. n.k

3 – ***Mujtahid Al Madhhab,*** kama Imam Al Buwaiti, ImamAl Rabi', Imam Al Anmati, Imam Al Ghazali n.k.

4 – ***Mujtahid Al Fatwa wa Al Tarjih,*** k.m. Imam Al Mawardi, Abu Tayyib, Al Tabari, Imam Al Haramayn, Imam Abu Ishaq Al Shirazi, Imam Al Ruyani, Al Rafi'i na Imam an-Nawawi.

5 – ***Al Hafizli l-Madhhab***na Mufti.

Imaam Al Nawawi amesema katika *Al Majmuu:* '**Iwapo mwenye kutoa hukumu katika madhhab ya Shafii ana nia ya kupendelea (kitu), haitajuzu kwake kujiegemeza kwenye kitabu kimoja au viwili tu vya kitabu. wasomi waliotangulia au hata vitabu vichache vya wanazuoni wa baadae kwa sababu ya tofauti kubwa katika maamuzi na matakwa yao. Ni jukumu la mufti huyu kueneza madhhab ya Imam Al Shafi'i *Radhi Allahu 'Anhu*.**

Hawezi kusadiki kwamba yaliyoelezwa katika vitabu hivyo ni Rai ya Imam Al Shafi'i au Rai anayoipendelea yeye mwenyewe kwa sababu ya rai mbalimbali, na jambo hili si geni kwa wale ambao wana ujuzi nao hata kidogo. Hivyo katika Madhhab kuna matukio ambapo waandishi kumi wanatoa maoni yanayokubalika juu ya mambo fulani, lakini ni ajabu kuhusiana na maoni yanayopendekezwa ya Madhhab na yanaenda kinyume na wengi. Wakati mwingine hata wanaenda kinyume na maandishi ya wazi ya Imam. Utaona baadhi ya mifano ya hili katika ufafanuzi huu, ikiwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* anataka. Natumai kwamba kitabu hiki kitakapokamilika, kitaweza kukidhi (na kutotosha) hakuna haja ya vitabu vingine na kitaunda Madhhab ya uhakika ya Imam Al Shafi'i, *Insha Allah Ta'ala*."*(Al Majmu' Sharh Al Muhadhdhab, 1:47)***

Imaam Al Kurdi amesema: **"Ikiwa Shaykhayn (Imam Al Nawawi na Imam Al Rafi'i) hapendelei (chochote), basi ikiwa Mufti ni wa *Ahl Al Tarjih,* anaweza kutoa hukumu kwa kuzingatia rai ambayo Maimam wa Madhhab yake wamejikita wenyewe. Haitojuzu kwake kutoa hukumu ambayo inachukuliwa kuwa dhaifu kwa mujibu wa Maimam wa Madhhab yake, hata kama hii ni Rai iliyopendekezwa kwa mujibu wake. Hii ni kutokana na ukweli kwamba yeye anaulizwa tu kuhusu rai iliyopendekezwa kwa mujibu wa Madhhab, si kwa mujibu wa nafsi yake, isipokuwa anaona udhaifu wa rai. Inafaa kuifanyia kazi Rai dhaifu wakati ameitangaza kuwa ni Rai dhaifu. Ikiwa yeye si katika watu wa *Tarjih*, na hawa ndio wanachuoni waliopo katika zama zetu, basi kuna maoni tofauti."**

Miongoni mwa watu muhimu baada ya Shaykhayn ni:

Imam Ibn Al Rif´ah, Al Subki na´alam Al khamsah: (1) Shaykh Al Islam Zakariyya Al Ansari, (2) Imam Al Shihab Al Ramli, (3) Imam Al Khatib Al Shirbini, (4) Imam Ibn Hajar Al Haythami, (5) Imam Al Shams Ad Din Al Ramli.

Inajulikana sana miongoni mwa Maulamaa wa baadaye wa Shafi'i kwamba walijiegemeza kwenye tafsiri mbili muhimu za Al Minhaj:

Tuhfat Al Muhtaj bi sharh Al Minhaj **kutoka kwa Imam Ibn Hajar Al Haytami (974 H)**

Nihayat Al Muhtaj ila sharh Al Minhaj **kutoka kwa Imam Shams Al din Al Ramli (1004 H)**

Fafanuzi hizi mbili zinapendekezwa kwa sababu ziliwasilishwa kwa mamia ya Maulamaa ambao walizichunguza na kuzithibitisha.

Maulamaa wote wa Misri, au angalau wengi wao, wamejikita kwenye hukumu za Imam Al Ramli alizozinukuu katika vitabu vyake, hususan katika Al Nihayah. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Al Nihayah ilisomwa kwa Imam na Maulamaa 400 na walikuwa wakikikosoa, kukichunguza na kukithibitisha kitabu hiki. Kwa hiyo, uthibitisho wake ulikuwa umefikia kiwango cha *Tawatur*.

Maulamaa wa Hadramawt, Sham, Akrad, Daghestan, Yemen na Hijaz walipendelea Rai ya Imam Ibn Hajar Al Haytami katika vitabu vyake kama Mu'tamad (nafasi ya kutegemewa), hususan *Al Tuhfah*.

Kutoka katika vitabu vya Al Imām Ibn Hajar, mpangilio wa sifa ni Al Tuḥfah, Fatḥ Al Jawād, Al Imdād, Al Fatawa(maoni ya kisheria) na *Sharh Alʿ Ubāb* vina sifa sawa, lakini kupendelea ufafanuzi ni bora zaidi.

Kwa hiyo, *Qawl Al Mutamad* ni Rai ya Shaykh ul Islami Imam Al Muhaqqiqin Ibn Hajar na Imam Shams Al Din Al Ramli *Rahimahum Allah Ta'ala.*

Imam '**Umar Al Basri, mmoja wa wanafunzi wakuu wa Imam Ibn Hajar, aliulizwa ni lipi linapaswa kupendelewa Zaidi pale panapotokea tofauti ya maoni kati ya Imam Ibn Hajar na Al Ramli. Hitimisho la jibu lake lilikuwa: 'Kama mwanachuoni angekuwa na fursa (huenda uwezo) wa kuangalia chanzo cha hukumu na ushahidi kwa hili, basi afanye hivyo na arejee kwenye dalili zilizotajwa na Shaykhayn au Wanazuoni wengine. Ikiwa hatapata fursa ya kufanya hivyo, basi achague baadhi ya Rai za Ibn Hajar au Al Ramli**.'

Ikiwa Maimam wawili hawa Ibn Hajar na Al Ramli *Rahimahumallah Ta'ala* hawakutoa hukumu juu ya mas-ala husika, basi fatwa itatolewa kwakulingana na mtizamo wa Shaykh Al Islam Imam Zakariyya Al Ansari katika *Sharh Al Saghīr ala Al Bahjah* na baada ya hapo, *Fath Al Wahhāb bi sharh Manhaj Al Tullab*, na mwishowe utaangaliwa kama ilivyotolewa katika Sharh Al Imām Al Khāṭib Al Shirbīnī.

Mpangilio wa sifa miongoni mwa Khawāsi (maoni ya pembeni) ni kama ifuatavyo: (Kutoka katika Al Fawaid na Al I'anah):

Imām Ali Ibn Yahya Al Ziyādī (1024 H), hāshiyah katika Fath Al Wahhab, maelezo ya Al Manhaj;
Imam Ahmad Ibn Qasim Al ʿAbbadi (994 H), katika Fath Al Wahhab;
Shihab Al Din Ahmad Al Burullusi anayejulikana kama ʿAmirah (957 H), maoni ya pembezoni juu ya Al Maḥalli;
Imam ʿAli Ibn 'Ali Al Shabramillisi (1087 H), maoni ya pembezoni kuhusu Al Nihāyah;
Imam Abu Al Hasan Ali Ibn Ibrāhīm Ibn Ahmad Al Halabī (1044 H), mwandishi wa Al Sīrah Al Halabiyyah;
Imam Muhammad Ibn Ahmad Al Shawbarī (1069 H), ana Hashiyyah kutoka kwenyeAl Mawahib Al Ladunniyyah na Hashiyyah huko Tahrīr Al Lubāb.

Imam Muhammad Ibn Dauud Al ʿAnānī (1098 H), ana Hashiyyah kutoka kwenye Al Tahrīr na Al Manhaj.

Maoni yao yanachukuliwa ikiwa hayatatofautiana na "*Al Tuhfah na Al Nihayah"* na kanuni za Madhhab.

Hivyo miongoni mwa Wanazuoni wenye Sifa ya As-hab Al Wujuh katika Madhhab ya Imam Al Shafii ni kama:
Imam Abu Yaqub Al Buwayti.
Imam Al Muzani.
Imam Abu Thawr.
Imam Al Rabi Ibn Sulayman.
Imam Al Zafarani.
Ambao hao wote ni Wanafunzi wa Imam Al Shafii, kisha baada yao unakutana na Wanazuoni kama:
Imam Ad Darimi.
Imam Ibn Al Mundhir.
Imam Al Anmati.
Imam Ibn Sura yj.
Imam Al Marwazi
Imam Al Isfarini.
Imam At Tabari.
Imam Al Shirazi.
Imam Al Juwayni.
Imam Al Haramayn.
Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali.
Imam Fakhr Ad Din Al Razi.
Imam Ibn Salah.
Imam Al Qaffal.
Imam Al Rafii.
Imam An Nawawi n.k.

Naam..tumefafanua kuhusiana na *As-hab al Wujuh* kwa sababu tuko kwenye Kufunga mikono ndani ya Sala na anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**As-hab (Al Wujuh) wetu Wanasema kua Sunna hua ni kuishusha chini mikono baada ya Takbir Al Ihram Na Kuuweka Mkono wa Kulia juu ya Mkono wa Kushoto, huku ukiwa umeukamata mkono wa kushoto kwenye kiunganishio cha kiganja chake na sehemu ya mbele zaidi baada ya kiganja kuelekea kwenye kisugudi.'**

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: **'Imam Al Qaffal amesema kua Mtu anaweza akachagua baina ya kunyoosha vidole vya Mkono wa kulia kuushika mkono wa Kushoto au kuvikunja huku akiushika mkono wa kushoto**. **Na Mikono inatakiwa iwekwe Chini ya Kifua na Juu ya Kitovu na huo ndio Mtizamo unaokubalika zaid.'***(Al Majmuu Sharh Al Muadhdhahab)*

Naam, Nadhani hapa itakua tumefahamiana kwanini Imam An Nawawi akasema As-hab wetu na kisha pia akamtaja mmoja kati ya As-hab hao ambae ni Imam Al Qaffal Al Shahi Al Marwazi.***(huyu ni Imam aliekua fundi mchongaFunguo na Kufuli na aliitwa Al Qaffal kwa sababu Qaffal ni Kufuli, Al Qaffal alikua fundi kufuli kwa mda wa miaka 40 na hivyo alikua hajui chochote kuhusiana na Ilm ya Dini, kwani alikua ni kama walivyo Maamuma wengi wa leo kua amemaliza Juzuu yake Amma basi, lakini kwa upande wa Al Qaffal basi alipotimia umri wa miaka 40 basi akaanza kutafuta Ilm Dini naAllah Subhanah wa Ta'ala akamfungulia milango ya ufahamu na kumjaalia Ilm kubwa sana kiasi ya kua***

kutokana na kukubalika kwake basi alifanikiwa hata kuhamishaSerikali ya Mamlaka ya Utawala wa Ardhi aliyokua akiishi kutoka kufuata Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa katika Sharia zake Kifiqh na kuanza kufuata Sharia za Fiqh za Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii, na Imam Al Qaffal akaishi kwa mda wa miaka 95 akiwa na Ilm kubwa sana ya kutisha hadi leo hii ambapomimi nawe tunamnukuuu kama alivyonukuliwa na Imam An Nawawi na Maimam wengine wengi)

Na katika kunukuu kwake Imam An Nawawi hakusema kua huu ni Mtizamo wa Imam Al Shafii.Bali kwanza kanukuu makubaliano ya As-hab Al Wujuh wa Madhhab ya Imam Al Shafii na kisha akajumuisha Ufafanuzi wa Imam Al Qaffal ambae ni *As-hab Al Wujuh* pia na akamalizia kusema kua : '**Na huu ndio Mtizamo unaokubalika zaidi**.' Yaani katika Madhhab ya Imam Al Shafii.

Hivyo Sunnah ya kufunga Mikono katika Wakati wa Kusali ni Sunnah iliyokua pia ikitekelezwa na wengi miongoni mwa Wanazuoni.Na imenukuliwa kutoka kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Said Ibn Jubayr, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Malik, Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii, Imam Abu Hanifa n.k

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Zayn Ad Din Al Sunayki Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Shafii kua: '**Hikma ya Kufunga Mikono na kuiweka Chini ya Kifua, ni kwa Sababu Kifua ndio Sehemu ya Kiungo cha Mwili ambayo ndani yake kuna Moyo ambayo Ndani yake ndio sehemu inayotoka Nia ya Kila kitu.Na hivyo basi hii (Ya kufunga Mikono chini ya Kifua) hua ni sawa na kama alivyosema Imam Al Qaffal kama ilivyonukuliwa kwenye Al Majmuu (ya Imam An Nawawi) na katika sehemu nyenginezo.**

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Shafii katika Kitab Al Umm basi yeye amesema kua Malengo ya Kuuweka mkono wa Kulia juu na kukamata Mikono wa kushoto hua ni kwenye kumsababishia Mtu kua ni mwenye kupata Utulivu, lakini kama mtu atapata utulivu zaidi akiiwachia basi hamna tatizo *(Al Iqna)*

Na ama tukirudi kwenye kauli ya Saad Ibn Sahl isemayo kua: '**Watu wameamrishwa kua Mtu aweke mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto katika wakati wa Kusali.'***(Imam Bukhari)*

Basi tunaona kua baadhi ya Wafuasi wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wameichukulia kauli hii kua hua Inamaanisha kua Kufunga Mikono Kulikozungumziwa hapa hua kunajumuisha Katika Sala nzima kila Unapokua katika hali ya Kisimamo ndani yake.

Na ndio maana basi unakuta baadhi ya watu hua Wanafunga pia mikono yao baada ya kutoka kwenye Rukuu kabla ya kuenda kwenye Sijda.Yaani baada ya maneno *Sami Allahu Liman Hamida* basi anafunga mikono kisha anafungua na kusema Allahu Akbar na kuelekea kwenye Sijda.

KUFUNGA MIKONO AU KUTOFUNGA BAADA YA RUKUU?

❖❖❖

عن محمد بن عمرو بن عطاء، قالسمعت أبا حميد الساعدي، في عشرة من أصحاب رسول الله : أنا أَعلمُكم بصلاة رسول الله صلى الله عليه :صلى الله عليه وسلم منهم أبو قتادة، قال أبو حميد

فَلِمَ؟ فوالله ما كنتَ بأكثرنا له تبعا ولا أقدمنا له :وسلم ، قالوا كان رسول الله صلى الله عليه وسلم إذا قام إلى الصلاة " :فاعْرِض، قال :بلى، قالوا :صحبة، قال يرفع يديه حتى يُحَاذِيَ بهما مَنْكِبَيْهِ ، ثم يُكبِّر حتى يَقِرَّ كل عظم في موضعه معتدلا، ثم يقرأ، ثم يكبِّر فيرفع يديه حتى يُحاذي بهما مَنْكبيه، ثم يركع ويضع رَاحَتَيْهِ على رُكبتيه، ثم يعتدل فلا يَصُبُّ رأسه ولا سمع الله لمن حمده، ثم يرفع يديه حتى يُحاذي بهما منكبيه معتدلا، ثم :يُقْنِعُ ، ثم يرفع رأسه، فيقول الله أكبر ثم يهوي إلى الأرض فيُجافي يديه عن جنبيه، ثم يرفع رأسه ويَثْني رجله اليسرى فيقعد :يقول الله أكبر، ويرفع رأسه ويَثْني رجله اليسرى :عليها، ويفتح أصابع رجليه إذا سجد، ويسجد ثم يقول فيقعد عليها حتى يرجع كل عظم إلى موضعه، ثم يصنع في الأخرى مثل ذلك، ثم إذا قام من الركعتين كبر ورفع يديه حتى يحاذي بهما منكبيه كما كبر عند افتتاح الصلاة، ثم يصنع ذلك في بقية صلاته حتى إذا كانت السجدة التي فيها التسليم أخر رجله اليسرى وقعد مُتَوَرِّكًا على شقه صدقت هكذا كان يصلي صلى الله عليه وسلم :الأيسر، قالوا

Kutoka kwa Muhammad Ibn Amr Ibn Ataa amesema kua: WakatiAbu Humayd Al Saadiakiwa amekaa na takriban Masabaha kumi *Radhi Allahu Anhum* wa *Rasul Allahu Alayhi wa Salam* akiwemo Abu Qatada*Radhi Allahu Anhu* alisema:

“Mimi ndiye mjuzi zaidi miongoni mwenu kuhusu (namna ya) sala ya *Rasul Allahu Alayhi wa Salam*.

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakauliza: Kwa nini? Wallahi wewe hukumfuata zaidi kama tulivyomfuata sisi, wala hukufuatana naye kabla yetu.’

Abu Humayd Al Saadi akasema ‘Hakika mimi ndie mjuzi zaidi.

Masahaba *Radhi Allahu Anhum*wakasema: ‘Basi tuonyeshe.’

Abu Humayd Al Saadi Akasema: ‘*Rasul Allahu Alayhi wa Salam* anaposimama Kusali, alikuwa akinyanyua mikono yake sambamba na mabega yake, akitamka Takbir, kisha anasubiri mpaka kila mfupa wa mwili wake utulie sawasawa. Kisha alikuwa akiisoma (Qur'ani), kisha anainua mikono yake sambamba na mabega yake na kusema Takbir, kisha akainama, akiweka viganja vyake juu ya magoti yake, kisha alikuwa akisimama wima akiinamisha kichwa chake bila kukiinua sana kisha anasema: '*Samia Allahu Liman Hamida'* kisha huinua mikono yake hadi usawa wa mabega yake huku akisimama wima Kisha husema Allahu akbar na, huku akiweka mikono yake mbali na ubavu wake, kisha anainua kichwa chake na kunyoosha mguu wake wa kushoto na kuukalia juu yake, na alikuwa akikunjua vidole vyake vya miguu wake wa kulia na hukaa hivyo mpaka kila mfupa urudi mahali pake. Kisha anaposimama baada ya Rakaa mbili, aliinua mikono yake hadi usawa wa mabega yake kama alivyokuwa akifanya mwanzoni mwa

Salah. Kisha alikuwa akimalizia sala yake iliyosalia kwa namna hiyo hiyo, na anapofika kwenye sijda inayofuatiwa na Taslim, alizogeza mbele mguu wake wa kushoto na kukaa, huku akiweka makalio yake upande wa kushoto juu ya ardhi."

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Umesema kweli; hivi ndivyo *Rasul Allahu Alayhi wa Salam* alivyokuwa akisali'*(Imam Abu Daud)*

Na amesema Abu Humaid As Saidi *Radhi Allahu Anhu* kua: **Nilimuona mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akitamka Takbirat Al Ihram, alikua akinyanyua Mikono yake hadi kufikia Mabegani Na anapo rukuu alikua akiweka Mikono yake kwenye Magoti yake; na kisha huupinda Mgongo wake(Kuunyoosha katika Rukuu): Na kisha anaponyanyua Kichwa chake Juu, husimama Sawasawa kiasi ya kua Mifupa ya Uti wa Mgongo wake hukaa Sawasawa.**

Anaposjudu huweka Mikono yake na kuonekana kua haikutanuka sana na wala haijajibana na Ncha za Vidole vyake huelekea Kibla. **Anapokaa mwishoni mwa Rakaa mbili, basi huukalia mguu wake wa Kushoto na kuusimamisha Mguu wa Kulia**. **Na anapokaa katika Rakaa ya mwisho huutanguliza mbele mguu wa kushoto na kuusimamisha wa kulia na kukalia Makalio yake***(Imam Bukhari)*

Naam..ingawa hii ni miongoni mwa Hadith ambazo zinaelezea nàmna ilivyokua akisali Sala zake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Lakini pia hii ni Hadith ambayo inatumiwa kama kithibitisho pia kwa pande zote mbili**za wale wasemao kua baada ya Kurukuu Hutakiwi Kufunga tena mikono kwani hadith imesema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua Akinyanyuka kutoka kwenye Rukuu hua ni mwenye kusimama sawia na kusimamisha Mifupa ya mwili wake wote.**

Na ingawa Hakuna Hadith Sahih inayosema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifunga mikono baada ya Kuja juu kutoka kwenye Rukuu lakini kwa wale wasemao kua Inatakiwa kufungwa mikono basi wao wanasema kua: **'Maneno ya Hadith hii yanamaanisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akitoka kwenye Rukuu basi alikua akirudisha hali ya Mifupa ya mwili wake kua kama ilivyokua hapo kabla ya Kuruku, na kwa kua baada ya kurukuu alikua amefunga mikono basi na hapa pia inabidi mtu afunge mikono.'**

Ambapo ukweli ni kua: '**Irsal yaani kuachia Mikono ndani ya Sala baada ya kutoka kwenye Rukuu ndio miongoni mwa vitendo vilivyonukuliwa katika Hadith Sahih za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam***. **Na hakuna hadith Sahih iliyosema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifunga Mikono baada ya kurukuu, na pia hakuna kauli ya Sahaba hata mmoja juu ya Jambo hilo,wala Tabiina aliefanya hivyo wala Tabii Tabiina.'**

Ambapo anasema Shaykh Rabi Al Madkhali ambae ni Shyakh wa Kisalafi kua: K**wa Hakika Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* ametaja katika Hadith yake hii baadhi ya Nguzo za Sala, Mambo ya Wajibu na yanayopendekezwa ndani yake, lakini hakutaja kuhusiana na kufunga mikono baada ya Kutoka kwenye Rukuu na kusimama, Na kuna Hadith za Masahaba kumi waliothibitisha Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama alivyothibitisha Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* ambapo hakuna hata mmoja miongoni mwao Masahaba hao aliesema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifunga mikono baada ya Rukuu.**

Na hata Shaykh Ibn Taymiyyah ambae pia ni Shaykh ul Islami wa Kisalafi amesema kua: '**Haipendekezwi Kufunga mikono baada ya kutoka kwenye Rukuu, kwa sababu kwanza Hakuna Hadith juu yake na kisha kwa Sababu katika wakati wa kutoka kwenye Rukuu hua**

hakuna mda mrefu ndani yake, kwani Mtu hua anajiandaa kuingia kwenye kwenye Sijda'*(Kitab Sifat Salat Min Sharh Al Umdah)*

Kwani amesema Imam Bukhari kua Amesema Abu Qilaba kua:**'Malik Ibn Huwairth alikua akitufahamisha sisi kuhusiana na Sala ya *Rasul Allah Salallahi Alayhi wa Salam* katika Nyakati ambazo zilikua si nyakati za Sala za Fardhi . Na hivyo alisimama na Kusali na akatekeleza Qiyam (Kisimamo)kisha akainama na Kurukuu kikamilifu, na kisha akanyanyuka na Kusimama Sawia kwa mda.'**

Abu Qilab anaendelea kusema kua: '**Malik Ibn Huwairith katika Kutuonesha na kuielezea Sala kwa vitendo alisali kama alivyosali Shaykh wetu Abu Yazid**. **Ambapo Abu Yazid alikua akikaa kwa mda kabla ya kunyanyua kichwa chake kutoka kwenye Sijda ya pili na kuja juu'***(Imam Bukhari)*

Na akasema Imam Thabit Al Bunani ambae ni Mwanafunzi wa Sahaba Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Anas aliua akitufundisha sisi Kusali kama alivyokua akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Na katika kutuonesha kwake basi alikua anaponyanyuka kutoka kwenye Rukuu alikua akikaa kwa mda kiasi ya kua tulikua tukidhania kua amesahau kuhusiana na Kusjudu'***(Imam Bukhari)***

Na amesema Imam Abd Rahman Ibn Abi Laila kua: **'Amesema Bara Ibn Azib kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisimama kwa mda kutoka kwenye Rukuu Na mda aliokua akitumia baina ya Sijda zake mbili ulikua ni sawa na mda aliokua akitumia kutoka kwenye Rukuu kuingia kwenye Sijda'***(Imam Al Bukhari)***

Naam, hizo ni baadhi ya Hadith zinazoelezea kuhusiana na Rukuu na Sujud za R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, ndani ya Sala na kama zinavyoonesha kua hakukuzungumziwa kuhusiana na Kukunja Mikono kifuani baada ya kurukuu.

Kwani ingawa Imam Ahmad Ibn Hanbal mwenyewe amekua katika hali ya kutokua na Uhakika wa Jambo hili na hivyo amesema: '**Kitendo cha kufunga Mikono baada ya Kurukuu ni kitendo ambacho hakijathibitishwa kwenye Sunnah lakini kama mtu akitaka basi na Aiachie Mikono, na akitaka basi na aifunge'***(Al Muharrara)*

Ambapo hii ni kauli ambayo imewapelekea Wanazuoni Wakubwa wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Hanbal kutolizungumzia Jambo hili na kuamua kutoligusa na kuachana kama lilivyo jambo hili miongoni mwao akiwemo Imam Ibn Muflih, Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi, Imam Al Buhuti, Imam Al Taghlabi, Imam Al Duwayyan, n.k kwani hawakusema kitu juu ya kuachia au kufunga Mikono baada ya Rukuu.

Lakini hata hivyo hali imekua tofauti kwa Mwanafiqh *Al Allamah* Imam Mari Al Karmi Al Hanbali wa Kisalafi basi yeye anasema kua: **Ni Sunna Kuachia Mikono Katika Kisimamo cha baada ya Rukuu kabla ya kusujudu** *(Dalil At Talib Li Nayl Al Matalib)*

TAWAJJUH –DUA IFTITAH AU DUA ISTIFTAAH

❖❖❖

Naam tuko katika kuzungumzia Sijdat As Sahw ambayo hutakiwa kutekelezwa baada ya Kuzidisha, Kupunguza kitu katika Sala au kua na Shaka juu ya kitu ndani ya Sala.Ambapo ili tuifahamu

utekelezwaji wake basi inabidi kwanza Tuijue Ibada nzima ya Sala.Na kama tulivyoahidiana kua malengo yetu ni Kufahamishana kila kitu tutakachojaaliwa kuweza kufamishana kuhusiana na Ibada ya Sala.

Na katika Kufahamishana kwetu basi bado tupo katika Nguzo ya Tatu ya Sala ambayo ni Qiyam yaani Kisimamo.Kwani ya kwanza ni Nia, kisha Takbirat Al Ihram na kisha ndio Qiyam.Ambapo kabla ya kuingia kwenye Nguzo ya Nne ambayo ni Qiraat Surat Al Fatiha yaani Kisomo cha Surat Al Fatih basi kabla yake hua kuna kuna kisomo kinachojulikana kamaDua Iftitah, Dua Istiftaah au Dua ya Ufunguzi wa Sala.

Ambapo pia hua inajulikana kama *Tawajjuh* yaani kuingia katika hali ya kuutafuta umakini wa kiakili na kiroho huku ukiwa umekielekea kitu ambacho kitakupatia uwezo wa nguvu inayokujaza Imani ndani ya Moyo na Roho, na hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Ibada ya Sala basi Tawajjuh hua ni Dua ya Ufunguo wa kuingia Sala wakati Mja akiwa amemuelekea Muumba wake yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na Ingawa kuna baadhi wanasema kua Dua hii inatakiwa kusomwa kabla ta Takbir al Ihram kiasi ya kua tunaona kua anasema Al Walid Ibn Muslim kua: '**Said Ibn Abd ul Aziz aliambiwaKua aliambiwa kua kuna Watu ambao walikua wakisema maneno ya Dua hizi kabla ya takbira ya ufunguzi, na akauliza Jee ni kina nani hao watu ambao imenukuliwa kutoka kwao?'** Ambapo mtizamo huu ulikua ni mtizamo wa Watu wa Mji wa Kufah nchini Iraq.

Na hii ni kwa sababu anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **Kila wakati baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutamka *Takbirat Al Ihram*, basi alikua anakaa kimyaa kabla ya kuanza kisomo chake(cha Surat Al Fatiha)Hivyo Siku moja nikamuuliza kwa kusema: Ya Rasul Allah! Baba yangu na Mama yangu watolewe Kafara kwa ajili yako Lakini mbona nakuona kua hua unakaa kimya baina ya *Takbirat Al Ihram* na Kisomo cha Surat Al Fatiha?'**

Hivi Jee hua unasema nini? Katika wakati huo?
***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu: Hua nnasema:**

اللَّهُمَّ بَاعِدْ بَيْنِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ، اللَّهُمَّ نَقِّنِي مِنَ الْخَطَايَا كَمَا يُنَقَّى الثَّوْبُ الأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ، اللَّهُمَّ اغْسِلْ خَطَايَايَ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ

Allahuma Baaid Bayni wa Bayna Khatayaya, Kama Baadta Bayna Al Mashriki wa Al Maghribi Allahuma Naqqini min Khatayaya kama yunaqqa ththawbu al abyadh mina Danas; Allahuma Ighsil Khatayaaya Bi Al Maai wa Thalji wa Al Baradi.

Tafsir: ***Ya Allah Niachie Huru kutokana na Dhambi zangu kama ulivyoachia huru baina ya Mashariki na Magharibi, Ya Allah nisafishe mimi kutokana na Dhambi zangu kama inavyosafishwa Nguo Nyeipe kutokana na Uchafu, Ya Allah Nikoshe kutokana na Dhambi zangu kwa Maji, Barafu na Theluji(****Imam Bukhari)***

Ambapo Dua Isiftaah pia inatumiwa na Wafuasi wa **Madhhab ya Imam Hanbal.**

Na amesema pia Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akianza Kusali basi alikua akisema:**

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ وَتَبَارَكَ اسْمُكَ وَتَعَالَى جَدُّكَ وَلاَ إِلَهَ غَيْرُكَ

Subhanak Allahuma wa bihamdika tabarakasmuka wa ta'ala jadduka wa la ilaha ghairuk

Tafsir: ***Utukufu ni wako Allah na Shukrani Zinastahiki kwako, Ya Allah Baraka ziwe Kwa Jina lako na Utukuke Ukuu wako, Hakuna anaestahiki kuabufiwa isipokua wewe****(Imam At Tirmidhii)*

Ambapo Maneno ya Dua ya Hadith ya Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu* ndio pia yaliyokua yakitumiwa na Amir ul Muuminin Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na Madhhab ya Imam Abu Hanifa kama ilivyoelezewa na Imam Muslim.

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Dua ya Ufunguzi wa baada ya kuingia ndani ya Sala basi ziko aina nyingi takriban 10 na hii ni kulingana na Hadith Sahih tofauti. Na Usomwaji wake hua ni Sunna *Mustahab* yaani Sunna inayotiliwa Mkazo isipokua kwa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik ambao wao wanasema kua haina haja ya kusoma *Dua Al Istiftaah.*

Ambapo pia kuna hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua: '**Wakati tulipokua tukisali na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mmoja miongoni mwa Watu alisema:**

اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا وَسُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلاً

Allahu Akbar Kabira wa Al Hamd Lillah Kathiran Wa Subhanah Allahi Bukratan wa Asila

Tafsir: **Allahu Ndie Mkubwa Zaidi, Shukran zote zinastahiki kwa Allah Na Utukufu ni wa kwake Asubuhi na Jioni'**

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: 'Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: 'Jee ni nani aliesema Maneno hayo?''

Yule Mtu akasema: 'Ni Mimi hapa Ya Rasul Allah!'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hakika mimi nimependezwa nayo na Milango ya Pepo ilifunguka kutokana nayo.'**

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* anasema: 'Tangu siku hio mimi sikuachana nayo maneno hayo'*(Sahih Muslim)*

Na pia kuna hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*ambayo inaonesha kua yeye alikua akisoma baada ya Dua Istiftah Dua ifuatayo:

اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا اللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا وَالْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا وَسُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلاً وَسُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلاً وَسُبْحَانَ اللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلاً أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ مِنْ نَفْخِهِ وَنَفْثِهِ وَهَمْزِهِ

Allahu Akbar kabiira, Allahu akbar kabiira, Allahu Akbar kabiira, walhamdulillahi kathiira, walhamdulillahi kathiiroa, walhamdulillahi kathiira, wa subhanallahi bukrataw waasilaa, wa subhanallahi bukratan wasilaa, wa Subhana Allahi Bukratan waasila a'udhu billahi minash shaitani min nafkhihi, wa naftshihi, wa hamzih.

*Tafsir:***Allah ni mkubwa, Allah ni mkubwa, Allah ni mkuu, sifa njema zote ni za Allah pekee, sifa njema zote ni za Allah pekee, na utukufu ni wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* Mchana na Jionina na utukufu ni wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* Mchana na Jioni na na utukufu ni wake *Allah Subhanah wa Ta'ala* Mchana na Jioni najikinga Kwako na Shetani aliyelaaniwa, na mnong'ono wake, na kuzomewa nae kwake, na mate yake**.***(Imam Abu Daud)*

Ama kwa upande mwengine basi tunaona kua Dua inayotumiwa na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Muhamad Idris Al Shafii niile yenye kutokana na Hadith ya Ali Ibn Abi *Talib Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua kila anapotaka kusali Sala ya Fardhi au ya Sunna basi baada ya kufanya Takbirat Al Ihram alikua akisoma Dua Istiftaah :

اللهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا وَالْحَمْدُ لِلهِ كَثِيْرًا وَسُبْحَانَ اللهِ بُكْرَةً وَاَصِيْلًاوَجَّهْتُ وَجْهِي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ حَنِيفًا، وَما أَنَا مِنَ المشْرِكِينَ، إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي، وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ العَالَمِينَ، لا شَرِيكَ له، وَبِذلكَ أُمِرْتُ وَأَنَا مِنَ المسْلِمِينَ،

Allahu Akbar Kabira W Alhamdulillaahi Kathiiraa, wa Subhaan Allahi Bukratan Wa'asillaa, Inni Wajjahtu Wajhiya lilladhi Fattara Samaawaati wal Ardha Haniifan Musliman wamaa Anaa Minal Mushrikiin. Inna Ssalaati wa Nusuki wa Mahyaaya wa Mamaati Lillahi Rabbil 'aalamiin. Laa Sharikalahu wa Bidhaalika Umirtu wa Ana Minal Muslimiin.

Tafsir: **Allahu Ndie Mkubwa zaidi, Shukran zote zinastahiki kwa Allah Na Utukufu ni wa kwake Asubuhi na Jioni**. **Kwa Hakika Mimi nnauelekezea Uso wangu kwa Allah, ambae ndie alieumba Mbingu na Ardhi ambavyo vyote ni vyenye utiifu na kujisalimisha juu yake**. **Na mimi si miongoni mwa wale wanaomshirikisha nae *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kwani Kwa Hakika Sala zangu, Ibada zangu, Maisha yangu, Mauti Yangu ni kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala tu. Ambae ni Mola wa Ulimwengu wote asiekua na Mshirika, Na hivyo ndivyo nilivyoamrishwa kufanya, na Mimi ni Miongoni mwa Waislam(waliojisalimisha kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala*).**

Anasema Imam An Nawawi kuhusiana na neno: **'Hanifa kua linamaanisha Kuelemea katika Kufuata njia ya muongozo wa Dini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* .'**

Na Imam Al Sanani anasema kuusiana na neon Nusuki kua linamaanisha '**Kua ni Ibadan a kila kitu kinachompelekea Mja kua karibu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* .'**

Na kama tulivyoona kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik, ni kua haina haja ya kuisoma Dua hio lakinikwa Upande wa tunaoisoma kulingana na vithibitisho vinavyoonesha kua ni Sunnah inayopendekezwa basi nadhani tunapoiangalia maana yake Dua hii hua tunaona pia Umuhimu wake na kujua kwanini ikahimizwa kusomwa, na ndani yake mna maneno ya Dua ya Nabii Ibrahim pia.

Tunaporudi katika Dua iliyonukuliwa na hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* basi tunaona kua: '**Maneno ya Dua yake yametokana na Hadithzilizo sahihi, ikiwemo hadithi hii ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu***'

‘Na tunaona kua Maneno ya Hadith yanatamkwapale mtu anapoanza Sala baada ya takbira: ‘Nimeelekeza uso wangu.’ Hii inaashiria wazi kwamba jambo hili halisemwi kabla ya Takbir al Ihram, bali baada yake na kabla ya kisomo. hivyo ni kabla ya takbir Al ihram.’

Ambapo kwa Hadithi ya Imam Muslim basi yeye amesema kua: **‘*Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Sala* alikua anasema pale anapoanza kusali, alikuwa akisema ‘Allahu Akbar’, kisha husema: ‘Ninaugeuza uso wangu..**’

Na kwa upande wa Imam Ibn Qudamah basi amesema kua: ‘**Na kwa kuwa kuifanyia kazi kumeachwa, hatumjui yeyote anayeitumia kama funguo, bali wao hutumia mwanzo wake.’** Na hili pialimethibitishwa na Imam Muhammad IdrisAl Shafi'i na As-hab Al Wujuh, Imam Ishaq Ibn Rahawayh, nk

Katika hadithi hii ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* tunaona pia kua maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Dua yake hii anaainisha kua: **‘Naelekeza uso wangu,’akimaanisha kua: ‘Naelekeza Ibada yangu na kuifanya kwa Ikhlasi kwa ajili ya *Allah Suhbahanh wa Ta’ala*, ambae ndie aliyeziumba Mbingu na Ardhi,na katika hayo yote mimi ni Mwenye kufuata Uongofu wake, na najiweka mbali na ushirikina ni mwenye kuelekea katika kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta’ala* , na muongofu ni miongoni mwa Wafuasi wa Hanifa yule aliye kwenye njia hii ya haki, ambae ni Nabii Ibrahim, ambae alikua katika Uongofu wa kufuata Imani ya Dini ya Kiislamu.’**

Kisha ndani yake Dua inaedelea kusema kwa kudhihrisha kua: “Sala yangu” ninayoiomba, na Sala jumuisho la pamoja la Dhikr, Kisomo cha Qu’an, Rukuu na Kusujudu, Dua na Tashahhud, na mambo mengine, “Na Sadaka yangu” ambayo ni Ibada, na kujidhibiti kwa kila kitu, na kichinjo changu kwa ajili ya kuupata ukaribu na *Allah Subhanah wa Ta’ala* na maisha yangu na kifo changu kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* .

Kwani *Allah Subhanah wa Ta’ala* ndie Muumba na Mmiliki wa kila kitu na mwenye kujua Majaaliwa ya Kila kitu, na hakuna mwengine mwenye mamlaka juu ya kila kitu zaidi yake asiekua na mshirika katika ufalme wake, na nimeamrishwa kufanya hayo yote. Kwa kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta’ala kwa* Ikhlasi katika kauli na imani, mimi ni miongoni mwa Waislamu waliojisalimishambele ya *Allah Subhanah wa Ta’ala* na kumnyenyekea kwa utiifu juu yakee, na ni mwenye kuzikubali sifa zote hizi za *Allah Subhanah wa Ta’ala*.

Ambapo katika sehemu nyengine ya Hadith basi tunaona kua katika Sala za Usiku hua kuna Dua Istiftaahi ambayo *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alikua akiiomba kwa kusema kaam ifuatavyo:

وجهت وجهي للذي فطر السماوات والأرض حنيفا مسلما وما أنا من المشركين، إن صلاتي ونسكي ومحياي ومماتي لله رب العالمين لا شريك له وبذلك أمرت وأنا أول المسلمين، اللهم

اللهم أنت الملك لا إله إلا أنت، أنت ربي وأنا عبدك، ظلمت نفسي واعترفت بذنبي فاغفر لي ذنوبي جميعها إنه لا يغفر الذنوب إلا أنت، واهدني لأحسن الأخلاق لا يهدي لأحسنها إلا أنت واصرف

عني سيىء الأخلاق لا يصرف عني سيئها إلا أنت، لبيك وسعديك والخير كله بيديك، والشر ليس إليك، أنا بك وإليك، تباركت وتعاليت أستغفرك وأتوب إليك

Allahu Akbar Kabira walhamdulillaahi kathiiraa, wa Subhaanallahi bukratan wa'asillaa, inni wajjahtu wajhiya lilladhi fattara Samaawaati wal Ardha haniifan musliman wamaa anaa minal mushrikiin. Inna ssalaati wa nusuki wa mahyaaya wa mamaati lillahi Rabbil 'aalamiin. Laa sharikalahu wa bidhaalika umirtu wa ana minal muslimiin.

Allahuma Anta al Maliku la Ilaha Illa Anta, Anta Rabbii wa ana Aabduka, dhalamtu Nafsi wa Aa'tarafat bi dhunubi faghfirlii Dhunubii Jamiaan innahu la yaghfir dhunuubi ila anta, wa hdnii al husni al khalaqa la yahdii lia ahsanha ila anta wa asrfi aAni sayian al akhlaq la yasrif aAni Saiyha ila anta. Labayka wa saadika wa alkhayr kulaha biyaddika wa al sharru laysa ilayka, anaabaki wa ilayka Tabarakta watawalayt astaghfiruka wa Atuubu Ilayk.

Tafsir: ***Nauelekeza uso wangu kwa aliyeziumba mbingu na ardhi, mwongofu na Mwislamu, wala mimi si miongoni mwa washirikina. Sala na ibada, uhai wangu na kufa kwangu ni kwa Mola Mlezi wa walimwengu wote, bila mshirika, na hivyo ndivyo nilivyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu. Wewe ni Mola wangu Mlezi na mimi ni mja wako, nilijidhulumu nafsi yangu na kukiri dhambi yangu, basi nisamehe madhambi yangu yote, hakuna anayesamehe madhambi isipokuwa Wewe, na niongoze kwenye maadili bora. Kwani hakuna anewaongoza wenye tabia bora isipokuwa Wewe.Na uniepushe na ubaya wa maadili.Hakuna awezaye kujiepusha na ubaya wangu.Bali Wewe.Furaha Yako na kheri Yako ziwe Kwako.Yote yamo mikononi mwako, na ubaya sio wako.Mimi ni mwenye kutokea kwako na kupitia kwako ndio utukufu ni wako, naomba msamaha wako na ninatubu kwako****.(Sahih Muslim)***

Ambapo ndani yake Dua hii kuna maneno yasemayo: '**Ya Allah, Wewe ndie Mfalme' yaani: Mmiliki wa kweli wa viumbe vyote, 'Na mimi ni Mtumishi wako' na hivyo Dua ni yenye kuthibitisha Kukiri kwa Mja kua*Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie Mfalme na Mmiliki wa kila kitu nikiwemo mimi mwenye kua wewe ndie Mmiliki na ni mwenye uwezo mkubwa sana wa kila kitu juu yangu na mimi ni mwenye kujidhulumu mwenyewe, na nilikubali hilo, kwani Nimeidhulumu nafsi yangu kutokana na kua ni mwenye kughafilika katika utekelezaji wa wa majukumu ya haki zako, na ninakubalia udhaifu wangu na makosa yangu, hivyo basi nakuomba nisamehe madhambi yangu yote kwani Hakuna anayesamehe dhambi isipokua Wewe.'**

Na kukiri huku kwa kukiri na kukiri uwezo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* wa kusamehe peke yake na kisha pia kukiri makosa yanayotokana na udhaifu na uzembe, hua ni katika hali hali ya juu ya Kuomba msamaha kwa heshima na adabu, kama walivyosema baba yetu na mama yetu Adam na Hawa pale ziliposema aya kua:

﴿قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَآ أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ﴾

Qala rabbana *dh*alamna anfusana wa-in lam taghfir lana watarhamna lanakoonanna mina alkhasireena *(Surat Al*Aaraf: 7:23*)*

Tafsir: ***Wakasema: Mola wetu Mlezi tumedhulumu. Na kama hutatusamehe na ukaturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa waliokhasirika."***

Kisha akasema, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*: 'Niongoze kwenye maadili mema na tabia njema,' Yaani Niongoze nikamilishe niwe na tabia bora kabisa, na uniwezeshe kuwa na tabia njema, na unijaalie niwe imara katika hayo, kwani Hakuna anaye muongoza kwa kiumbe kua mbora wao isipokuwa Wewe. Mkononi mwako tu upo uwongofu, na kwa hakika Nyoyo za waja ziko baina ya kidole chako. Kutokana na vidole vya Mwingi wa Rehema huwageuza apendavyo. 'Na uniepushe na ubaya wake.' maana yake: niweke mbali nami mambo yote mabaya na yenye kuchukiza.'Hakuna awezae kuniepushia ubaya wake isipokuwa Wewe.' na huku ni mwenye kukiri kwamba *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndiye pekee anaeweza kuiondoa amri hiyo na kuwaepusha na waja Wake ubaya wake.

Kisha akasema, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*: kua'Mimi niko chini ya amri yako.'yaani Nitaendelea kutii na kutii amri yako mara kwa mara na Nitasimamia. Na kufuata dini yako baada ya kufuata, 'Na kheri zote zimo mikononi mwako.' maana yake: kukiri kwamba wema wote Inawafikia waja na kufika kwake kunatarajiwa, kwani iko mikononi mwa Mola Mtukufu. 'Haukukuhusu wewe ubaya' kwa hivyo uovu hauwezi kuhusishwa na wewe, au ubaya hauwezi kukukaribia. au ubaya haupandi kwako. Bali, maneno mazuri ni yale yanayopanda juu. Kisha akasema: 'Kufaulu kwangu kuko Kwako, kimbilio langu, na kuwepo kwangu kunatokana na wewe, na kuwepo kwangu ni kwa kukutafuta Wewe, na marejeo yangu ni Kwako, au Kwako nakimbilia hifadhi yako.

Na Utukufu ni Wake*Allah Subhanah wa Ta'ala* , ni aliye juu zaidi katika sifa zake, Aliye Juu Zaidi Yake Mwenyewe juu ya viumbe vyote, na kutukuka kwake, Utukufu ni Kwake. Kisha akasema: 'Nakuomba msamaha na ninatubu Kwako," maana yake: 'Ninakuomba. Msamaha unifutie madhambi yangu.'

Hivyo Dua ya ya *Al Isiftitaah* hua ni Dua inayopendekezwa kwa kila anaesali, iwe ni Imam au Maamuma iwe katika Sala ya Fardhi au katika Sala ya Sunna, baada ya *Takbirat Al Ihram* kabla ya kutamka *Taawudh* inayofuatiwa na kisomo cha*Surat Al Fatiha.*

AT TA'AWWUDH –AUDHU BILLAHI MINA AL SHAYTANI RAJIIM

❖❖❖

Neno *Ta'awwudh* linatokana na neno A'udhuambalo hua Si Amrisho wala si Pendekezo au Ushauri bali hua ni Ombi lililojaa Unyenyekevu Kamilifu ndani yake kutokana na Udhaif wa anaeomba maombi ya kupatiwa Ulinzi au hifadhi dhidi ya kitu fulani kutoka kwa anaemuomba.

Ambapo ndani ya Maana ya Neno hili basi Anaejipendekezesha kwa ajili ya kutafuta Ulinzi au Hifadhi au Ukimbizi kwa Unyenyekevu kamilifu kutokana na Udhaifu wake hua si Mwengine isipokua ni Kiumbe yaani Ibn Adam kwa Mola wake.

Na tunapozungumzia neno Au'udhu basi Ndio lililotoa neno Istihadhah ambalo hua linamaanisha kuomba Ulinzi ama hifadhi huku muombaji akiwa katika hali ya Unyenyekevu wa hali ya Juu. Na amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Surat An Nahl kua:

﴿فَإِذَا قَرَأْتَ ٱلْقُرْآنَ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَانِ ٱلرَّجِيمِ﴾

Fa-idha qara/ta alqur-ana faistaAAidh biAllahi mina alshshaytani alrrajeemi*(Surat An Nahl 16:98)*

Tafsir: Na ***Hivyo MtakaposomaQur'anBasi Ombeni Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.***

Na Wanasema Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua**: 'Aaya hii ilishushwa kuhusiana na wale ambao walikua wakisali wakati ambao kuna kisomo cha Imam katika Sala'** ambapo miongoni mwao ni Abd Allah Ibn Masud, Abd Allah Ibn Abbas na Abd Allah Ibn Mughaffal *Radhi Allahu Anhum.*

Kumaanisha kutakiwa kuomba ulinzi kutoka kwa *Allah Subhanah wa Taala* kwa ajili ya kujikinga dhidi ya Shaytani Alielaaniwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua kunatekelezwa Wakati mtu akiwa tayari ameshaingia ndani ya Sala ameshatia Nia, amesha sema Allahu Akbar na tayari amesha omba Dua ya Ufunguzi wa Sala, na hivyo kabla ya kuanza kusoma Aya za qur'an za Surat Al Fatiha basi Kama zilivyo amrisha Aya za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua kabla ya Kusoma Quran basi tunatakiwa kusema *Audhu Bi Allahi Minna Al Shaytani Al Rajiimi.*

Na hii ni kwa sababu kama anavyoelezea *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika aya zinazfuatia baada ya hio kua:

﴿إِنَّهُ لَيْسَ لَهُ سُلْطَانٌ عَلَىٰ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ۝ إِنَّمَا سُلْطَانُهُ عَلَىٰ ٱلَّذِينَ يَتَوَلَّوْنَهُ وَٱلَّذِينَ هُم بِهِۦ مُشْرِكُونَ﴾

Innahu laysa lahu sultanun AAala alladhiina amanoo waAAala rabbihim yatawakkaloona; Innama sultanuhu AAala alladheena yatawallawnahu waalladheena hum bihi mushrikoona.*(Surat An Nahl 16:99-100)*

Tafsir: ***Kwa Hakika (Shaytan) hana uwezo mbele ya Waumini (Wanaomuamini Allah Subhanah wa Ta'ala) na wakawa ni wenye kuymtegemea Mola wao. Uwezo wake (Shaytan) ni kwa wale tu ambao ni wenye kumfuata na kumtii yeye na wale wanaomshirikisha Allah Subhanah wa Ta'ala .***

Na ingawa inaweza ikaonesha kwamba kwa kua hua tunatakiwa kusoma Qur'an katika Kisimamo cha Kila Rakaa, basi labda huenda ikawa kila tukitaka kusoma basi inabidi tuanze na Istihadhah, lakini hata hivyo Istihadhah hua inatakiwa kusomwa mara moja tu, ambayo ni katika Rakaa ya Kwanza tu, na hii ni kulingana na Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni.

Na hii ni kwa Sababu mbali ya Kua Sala husika inaweza ikawa na Rakaa mbili, Tatu na Nne lakini tunapozungumzia Usomwaji wa Qur'an ndani ya Sala hua unahesabika kua ni Usomaji mmoja tu, yaani kisomo hua kinahesabiwa kama vile ambavyo mtu atakaa kisha achukue Msahafu aanze kusoma Surat Al Fatiha, kisha Surat AlIkhlas, kisha Surat Al Baqara n.k

Ambapo katika hali kama hii basi Mtu huyu anaesoma Qur'an hua hatakiwi kua akisoma Surat Al Fatiha basi Aanze na Audhu Bi Allahi minna Al Shaytani Al Rajiim, kisha akishafika *Ghayri Al Maghdhuubi aalayhim wala Dhaaliin..*Aamin.

Kisha aanze tena *Audhu Bi Allahi Minna Al Shaytani Al Rajiim* kisha ndio aanze kusoma Surat Al Ikhlas na akimaliza basi arudie tena *Audhu bi Allahi minna Al Shaytani Al Rajiim* kisha aanze Surat Al Baqara.

La haiwi hivyo bali hua anasoma Taawidh mara moja tu hata asome Sura ngapi tofauti au msahafu mzima kwani kisomo chake hua kinahesabiwa kua ni kisomo kimoja.Ambapo na hivyo hivyo ndivyo kinavyohesabiwa kisomo cha ndani ya Sala, hua ni kisomo kimoja tu, na huu ndio mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Abu Hanifa

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi Taawudh hua haina haja kuisoma katika Sala za Fardhi lakini unaweza ukaisoma kwenye Sala za Sunna..

Ambapo maneno haya ya Taawidh hua pia ni Sunna Inayotiliwa Mkazo.Kwani ni pendekezo kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuna baadhi ya wakati alikua anapoanza kusoma Qur'an basi alikua hafanyi Istihadhah bali alikua anaanza moja kwa moja na Bismi Allahi na baadhi ya wakati anaanza na Istihadhah.

Ambapo katika Kitabu cha Sahih Muslim na Sahih Bukhari basi kuna hadith zisemazo kua*:* ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alikua kila akisimama kwa ajili ya kusali sala ya kablia ya Salat Al Fajr basi alikua akifanya IstiaAadha kwa kusema:** ***Aaudhu Bi Allahi Al Samiaun Al Alimun Mina Al Shaytani Al Rajiimi - Naomba Hifadhi kwa unyenyekevu kutoka kwa Allah mwenye Kusikia kila kitu na mwenye*** **kujua kila kitu, dhidi ya Shaytan alielaaniwa au aliefukuzwa kutoka kwenye Rehma zake Muumba.'**

Na vile vile kuna Hadith isemayo kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alikua anaposali hua ni mwenye kusema: Akisema** ***Audhu Bi Allahi Al Samiun Al Alimun min Ash Shaytani ArRajiim wa Nafkhihi wa Nafthihi.*****(***Imam Abu Daud)*

Ambapo hii pia ni aina nyengine ya Istihadhah na hivyo basi inaruhusika kutumia moja kati ya aina hizi ndani ya Sala pale unapoingia ndani ya Sala kabla ya kusoma Surat Al Fatiha ya Rakaa ya Kwanza.

Ama kwa upande wa Imam Hasan Al Basr, Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Ibn Hazim, Shaykh Ibn Taymiyyah n.k basi wao wanasema kua: '**Taawidh hua inajietegemea kwa hivyo hua inatakiwa kusomwa katika Kila Rakaa ya Sala Husika.'**

Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafiikama anavyosema Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii Al Tusi kua: '**Mtu anaposali baada ya Dua ya Istiftahi basi hufanya Taawudh kwa kusema:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa. **kisha anasoma Surat Al Fatiha kwa kuanzia na Bismillahi**' Hujjat Ul Islami akaelezea Rakaa ya mwanzo yote kisha akasema: '**Na huu ndio Mwisho wa Vitendo na Kauli za Rakaa ya Kwanza, na hivyo baada yake atafuatishia Kusali Rakaa ya pili kwa kuanza na Taawudh.'**

Na hii ndio Taawidh inayokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii, kwani kama tulivyosema kua Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Al Ghazali ni As-hab Al Wujuh na ni mwenye Sifa ya

Mujtahid.Na mwenye sifa ya kua na uwezo wa kuanzisha Madhhab yake mwenyewe lakini hata hivyo aliamua kufuata Madhhab ya Imam Al Shafii.

Kwani anasema Imam Muhamamd Idris Al Shafii kua: '**Mimi hua nnapendelea zaidi kusema:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Na Ingawa kila kauli yenye kuonesha kuomba hifadhi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi ya Shaytan hua inatosheleza.*(Kitab Al Umm)*

Hivyo ingawa kuna aina tofauti za Taawudh lakini kwa upande wa Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii basi yeye anasema kua**: 'Ingawa kila Kauli yenye kuonesha kuomba Hifadhi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi ya Shaytani hua inatosheleza lakini mimi hua nnapendelea zaidi:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.'*(Kitab Al Umm.)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Abu Ibrahim Al Muzani Al Shafii nae amesema pia kua**: 'Kisha baada ya Dua ya Istiftahi basi Omba hifadhi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi ya Shaytani kwa kusema *:***

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa..'*(Mukhtasar Al Muzani)*

Na akasema Al QadhiImam Abu Muhammad Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Baghawi na Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Al Mawardi Al Shafii kua: '**Kisha baada ya Dua ya Istiftahi basi Omba hifadhi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* dhidi ya Shaytani kwa kusema *:***

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.'(*Al Iqna*)

Na katika kitabu chake cha Al Hawi Al Kabir basi Al Qadhi Imam Abu Muhammad Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Baghawi na Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Al Mawardi Al Shafii kua anaendela kusema katika sehemu nyengine kua: **Ambapo**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Ndio inafaa na kuendana zaidi kuliko kusema Ghawiyyi na ni bora zaidi kusema kuliko kusema*: Audhu Bi Allahi Al Samii Alimi mina Shaytani Rajiimi* Na hii ni kwa sababu *Allah Subhanah wa*

Ta'ala **amesema katika Quran kua:*Audhu bi Allahi Aliyyi mina Al Shaytani Ghawiyyi* na kusema *Audhu Bi Allahi Mina Al Shaytani:***

﴿فَإِذَا قَرَأْتَ ٱلْقُرْآنَ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَانِ ٱلرَّجِيمِ﴾

Fa-idha qara/ta alqur-ana faistaAAidh biAllahi mina alshshaytani alrrajeemi.'*(Surat An Nahl 16:98)*

Tafsir: ***Na Hivyo Mtakaposoma Qur'an Basi Ombeni Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.***

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi kua: Amesema Imam Abu Is-haq Al Shirazi kua: **'Kisha baada ya Dua ya Ufunguzi basi Mtu anatakiwa aseme:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Ama kuhusiana na Hadith ya Abu Said Al Khudri ***Radhi Allahu Anhu*** **isemayo:**

أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ مِنْ هَمْزِهِ، وَنَفْخِهِ، وَنَفْثِهِ

Auudhu bi Allahi Samii Alim mina Al Shaytan Rajiim wa Nafkhihi wa Nafthihi

Ambayo Imam Abu Daud ameinukuu kwanye Sunan yake ni hadith ngeni, Na uthibitisho unaokubalika katika Madhhab yetu ni utokanao na kauli ya ***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **pale aliposema:**

﴿فَإِذَا قَرَأْتَ ٱلْقُرْآنَ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَانِ ٱلرَّجِيمِ﴾

Fa-idha qara/ta alqur-ana faistaAAidh biAllahi mina alshshaytani alrrajeemi*(Surat An Nahl 16:98)*

Tafsir: Na ***Hivyo Mtakaposoma Qur'an Basi Ombeni Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.***

Na hivyo huu ndio msimamo sahih kulingana na maana ya Aya.'

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Na Amesema Imam Al Shafii katika Al Umm na pia wamesema** ***As-hab Al Wujuh*** **wetu kua: Taawudh inatakiwa kutumika katika kila sehemu inayohitajika*Istihadhah* kutoka kwa Allah kwa ajili ya Kujikinga Dhidi ya Shaytan, na Taawudh iliyobora zaidi na yenye nguvu zaidi ni:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.*(Al Muhadhdhab)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi anaendelea kusema kua: **'Ama kuhusiana na**

'أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

'A'udhu bi-Llah is-Sami' il-Alim min ash-Shaytan ir-Rajim basi hii ni fatwa ya Imam Abū Bishr Al Yamān Ibn Abī l-Yamān Al BandanījīnaImam ad-Din Abu Al Qasim Abdul Karim Ibn Muhammad Ibn Abdul Karim Ibn Al Fadhl Ibn Al Hasan ar-Rafi'iameinukuaa ambapo nayo hii pia ni Ngeni.

Ambapo kwa upande wa Imam Al Ḥasan Ibn Ṣāliḥ Ibn Hayy Al Hamdani alikua akisema:

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ إنَّ الله هو السميع العليم

'A'udhu bi-Llah is-Sami' il-Alim min ash-Shaytan ir-Rajim

Na Imam Abu Bakr Al Qaffal Al Kabir ash-Shashi amenukuu kutoka kwaAl Hasan Ibn Salih kua alikua akisema:

أَعُوذُ بِاَللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ إنَّ اللَّهَ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

'A'udhu bi-Llah is-Sami' il-Alim min ash-Shaytan ir-Rajim, Inn Allahu huw as-Sami' ul-Alim'.

Na Imam At Tirmidhi amenukuu kutokea kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal ambae katika kutegemea kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* isemayo;

﴿وَإِمَّا يَنزَغَنَّكَ مِنَ ٱلشَّيۡطَانِ نَزۡغٞ فَٱسۡتَعِذۡ بِٱللَّهِ إِنَّهُۥ سَمِيعٌ عَلِيمٌ﴾

Wa-imma yanzaghannaka mina alshshaytani nazghun faistaAAidh biAllahi innahu sameeAAun AAaleemun.*(Surat Al Aaraf 7:200)*

*Tafsir: **Na Kama ukikujieni mnong'onezo muovu wa Shaytani basi ombeni Hifadhi kutoka kwa Allah kwani kwa hakika yeye ni mwenye kusikia kila kitu na ni mwenye kujua juu ya kila kitu.***

Hivyoanasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: **'Taawudh katika kila Rakaa ndio Msimamo wa Madhhab yetu, ndio Qawl Al Mutammad – Inayokubalika'***(Minhaj Al Talibin)*

Kwani kwa Imam ambae Wanazuoni wamekubaliana kua Mtizamo wake ni Sahih juu ya Jambo hili ambae si mwengine isipokua Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii ambae anatubainishia kuhusiana na Hukmu ya Taawidh ndani ya Sala kwa kusema kua: '**Kama Mtu ataiaacha kuisoma Istihadhah:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

(Audhu Bi Allahi Mina Al Shaytani Al Rajim baada ya Dua ya Ufunguzi wa kuinga ndani ya Sala na kabla ya Surat Al Fatiha) **kutokana na Kuisahau, kutokujua au kwa makusudi,basi haitokua na haja kwake kuirudia au kuitekelezea Sijdat Sahw kwa ajili yake.'**

Imam Al Shafii anaendelea kusema kua: **'Na mimi sipendelei kua Mtu aiwache kwa makusudi, na hua napenda kua mtu aisome katika Rakaa ya kwanza na katika Rakaa zitakazofuatia.'**

Imam Muhammad Idris Al Shafii anaendelea kutuambia kua: '**Ama kwa Hakika kile kilichonizuia mimi nisiwalazimishe watu kuirudia Istihadhah ni kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomfundisha Mtu kusali basi alimwambia asome kile anachokiweza kitakachomtosheleza katika Sala, na hakumuamriaha mtu Kusoma Taawidh na hivyo hii inaonesha kua Sala ya Mtu haitoharibika kama itakua hakusoma *Taawidh'*** *(Kitab Al Umm)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi kua: **'Kwa hakika Taawidh ni Mustahab na hivyo sio kitu cha lazima, ila hua ni Mustahab (kinachoendekezwa) kwa kila anaesoma Qur'an iwe yuko ndani ya Sala ama nje yake, na hukmu yake ni kuisoma katika kila Rakaa hua ni Mustahab kulingana na mtizamo unaokubalika wa Madhhab yetu, ambapo Mtizamo wa pili ni kua hu ni Mustahab kuisoma katika Rakaa ya kwanza tu, na hivyo kama mtu akiisahau kataika rakaa ya kwanza basi anaweza kuisoma katika Rakaa ya pili**'*(Al Tibyaan fi Ada Hamalah Al Quran)*

Ambapo anasema Imam Muṣṭafā Dīb Al Bughā Al Maydānī ad-Dimashqī ash-Shāfiʿī kua : **'Malengo ya kupendekezwa kusoma Taawidh katika kila Rakaa hua ni kutofautisha baina ya Kisomo cha cha Rakaa ya kwanza na visomo vya Rakaa zinazofuatia**'(*Ifadah Al Raghibin Sharah Minhaj Al Thalibin, Al Bugha)*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Did, Sultan Al Mutakkalimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi anasema kua: '**Kuna wasemao kua 'Taawudh inatakiwa isomwe baada ya kumaliza kisomo cha Qur'an' ambapo huu nimtizamo wa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu,* Imam Muhammad Ibn Sirrin na Imam Ibrahim AnNakhai'**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Jafar Muhammad Ibn Jarir Ibn Yazeed Ibn Kathir Ibn Galib Ibn Jarir At Tabari katika kuitafisiri aya ya 98 ya Surat An Nahl isemayo:

﴿فَإِذَا قَرَأْتَ ٱلْقُرْآنَ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَانِ ٱلرَّجِيمِ﴾

Fa-idha qara/ta alqur-ana faistaAAidh biAllahi mina alshshaytani alrrajeemi*(Surat An Nahl 16:98)*

*Tafsir: Na **Hivyo Mtakaposoma Qur'an Basi Ombeni Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.***

Basi anasema kua: **'Maneno haya hayamaanishi kua hili ni amrisho bali ni pendekezo, na hii ni kwa sababu kulingana na Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni ni kua hua hakuna makosa kwa mtu kusoma Qur'an bila ya kuanza na Taawidh, au baada yake na hivyo mtu huyo hua kamwe hahesabiki kua ni mwenye kudharau jambo la Fardhi au la Wajib.'***(Tafsir Al Tabari)*

Ambapo kwa upande wa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Sahl Abu Bakr Al Sarkhasi Al Hanafi anasema kuhusiana na maneno ya Taawidh kua: '**Ama**

miongoni mwa Wasomaji wa Qur'an basi kuna tofauti ya mitizamo katika kufanya Taawudh, kwani Al Qarri Abu Amr, Al Qarri Asim na Al Qarri Ibn Kathir wanaipendelea zaidi kutumia

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Ambapo wasomaji kutoka Al Hubayrah basi wao hupenda kutumia:

أَعُوذُ بِاَللَّهِ الْعَظِيمِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

.

Audhu Bi Allahi Al Adhimi Al SamiiAiy Al Aalimi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Mtukufu na mwenye kusikia kila itu na mwenye kujua ju ya kila kitu Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Na Qarri Nafii, Qarri Umir *na Qarri* Al Kisai hupenda kutumia:

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم إِنَّ اللَّهَ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Rajiimi Inna Allaha Huwa Al Samiiu Al Alimun – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah dhidi ya Shaytani alielaaniwa, hakika yeye Allah ni mwenye kusikia na ni mwenye kujua juu ya kila kitu.

Na Al Qarri Hamza Al Zayyat basi hupenda kutumia:

أَسْتَعِيذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

Istaidhu Bi Allahi mina Al Shaytani Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Na huo ni mtizamo wa Imam Muhammad Ibn Sirin.*(Al Mabsut)*

Na anasema Allamah Abu Bakar Alaa Din Ibn Masud Al Kasani Al Samarqandi Al Hanafi kua: **'Ama kuhusiana na namna inavyotakiwa kusema katika Taawudh basi inavyopendekezwa ni kusema:**

أَسْتَعِيذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

IstaAidhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Au kusema:

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Kwani kilichobora hua ni kile kinachotokana na maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake na maneno haya mawili yametokana na kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Na hivyo haina haja ya kuongezea maneno mengine zaidi yake kwa mfano kama:

السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

Al Samiun Al Alimun – Mwenye Kusikia na Kujua juu ya Kila kitu.*Kwa sababu ongezeo hili hua ni katika kiutukuzo(Bidai Al Sanai)***

Ambapo kwa upande wa Imam Burhan Ad Din Mahmud Ibn Ahmad Ibn Mazah Al Hanafi nae amesema hivyo hivyo na kisha akaongezea kwa kusema**: 'Na Mja anapotaka kuomba hifadhi, basi kile kinachoendana na Qur'an kuhusiana na hili hua ni:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

***Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa, na kama akisema Audhu Bi Allahi Al Adhiim au Audhu Bi Allahi Samiun Alimun,* basi hua ni mwenye kutofautisha baina ya *Taa'wudh* na Kisomo wakati kunatakiwa kuwe na umuhimu wa kisomo kua ni chenye kushikamana na Taawudh**.'*(Muhit Al Burhan)*

Ambapo kwa upande wa Imam Fakhr Ad Din Abu Umar Uthman Ibn Ali Al Zaylai Al Hanafi basi yeye anasema kua: **'Na miongoni mwa namna za kufanya*Istihadhah*hua ni kusema:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

***Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.* Ambapo hii ndio *Taawudh* inayopendelewa zaidi na Hamza miongoni mwa Wasomaji wa Qur'ani kutokana na kua ni yenye kukubaliana na maneno ya Qur'an na ndio pendekezo la *Shams Al Aimaah*pia ni kusema:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.*(Tabayyin Al Haqaiq)*

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Muhammad Mahmud Ibn Ahmad Ibn Musa Badr Ad Din Al Ayni Al Hanafi basi yeye anasema kua: '**Na Wasomaji wa Qur'an wametofautiana kuhusiana na maelezo ya Istihadhah, lakini Al Qarri Abu Amr, Al Qarri Asim, Al Qarri Ibn Kathir basi wao wanapendelea:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

***Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.*Watu wetu pia na Imam Al Shafii ameandika kua Istaidhu hii ndio bora zaidi, na pia huo nido mtizamo wa wengi miongoni mwa wenye Ilm**.(*Al Binayah Sharh Al Hidaya)*'

Na akasema Imam Abu Ikhlas Hasan Ibn Ali Al Shurunbulali Al Hanafi basi anasema kua: **'At TaAwudh hua ni Mtu kusema:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa*. Na ndio mtizamo thabiti unaokubalika katika Madhhab yetu.(Maraqi Al Falah)***

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi tunaona kua anasema Imam Shihab Ad Din Al Qarafi Abu Abbas Ibn Ahamad Ibn Abi Ala Idris Ibn Abd Rahman Ibn Abd Allah Ibn Yallin Al Sanhaj Al Saidi Al Bahfashimi Al Bushi Al Ahnasi Al Misri Al Qarafi kua: **'Taawudh hua ni kusema:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.'*(Adh Dhakirah)*

Ambapo kwa upande wa Abu Abdallah Muhammad Ibn Ahmad Muhammad Ulaysh katika *Minh Al Jalil Sharh Ala Mukhtasar* Sayyid Al Khalilbasi nae anasema kua: '**Na Taawudh maana yake ni:**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.'

Na anasema Imam Ibn Qudāmah Al Maqdisī Muwaffaq ad-Dīn Abū Muḥammad ʿAbd Allāh Ibn Aḥmad Ibn Muḥammad Al Hanbali kua: **'Maana ya Istihadhah hua ni kusema**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.'

Na huo ndio mtizamo wa Imam Abu Hanifa na Imam Al Shafii kutokana na maana ya maneno ya Aya ya 98 ya Surat An Nahl isemayo:

﴿فَإِذَا قَرَأْتَ ٱلْقُرْآنَ فَٱسْتَعِذْ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيْطَانِ ٱلرَّجِيمِ﴾

Fa-i<u>dha</u> qara/ta alqur-<u>a</u>na faistaAAi<u>dh</u> biAll<u>a</u>hi mina alshshay<u>ta</u>ni alrrajeemi*(Surat An Nahl 16:98)*

Tafsir: ***Na Hivyo Mtakaposoma Qur'an Basi Ombeni Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.***

Ambapo kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal ni kusema:

أَعُوذُ بِاَللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi Al SamiiAiy Al Aalimi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Mwenye kusikia Kila kitu na Mwenye kujua juu ya kila kitu Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.

Kwa mujibu wa Hadith ya Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu* na kwa mujibu wa maneno ya *Allah Subhanah wa Taala* katika Quran pale aliposema:

﴿ وَإِمَّا يَنزَغَنَّكَ مِنَ ٱلشَّيۡطَٰنِ نَزۡغٞ فَٱسۡتَعِذۡ بِٱللَّهِۖ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ﴾

Wa immaa yanzaghannaka minash Shaitaani nazghun fasta'iz billaahi innahoo Huwas Samee'ul 'Aleem*(Surat Fusilat 41:36)*

Tafsir: ***Na ikikujieni dhana mbaya kutoka kwa Shetani, basi jikinge kwa Allah Subhanah wa Ta'ala . Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.***

Na ainazote hizi ni zenye kujumishwa kua ni sawa na yeyote yule atakaeitumia kwa ajili ya kutafuta *Hifadhi ya Allah Subhanah wa Ta'ala* basi atatekelezewa haja yake.*(Al Mughni)*

Ambapo kwaupande wa Imam Muhammad Ibn Al Najjar Al Futuh Al Masri Al Hanbai basi yeye anasema kua: **'Kuomba Istihadhah hua ni kusema**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.'

Kutokana na maana ya maneno ya Aya ya 98 ya Surat An Nahl isemayo:

﴿فَإِذَا قَرَأۡتَ ٱلۡقُرۡءَانَ فَٱسۡتَعِذۡ بِٱللَّهِ مِنَ ٱلشَّيۡطَٰنِ ٱلرَّجِيمِ﴾

Fa-i<u>dha</u> qara/ta alqur-<u>a</u>na faistaAAi<u>dh</u> biAll<u>a</u>hi mina alshshayt<u>a</u>ni alrrajeemi*(Surat An Nahl 16:98)*

Yaani kufanya Istihadhah pale unapotaka kusoma Qur'an na Istihadhah hua ni yeyote ile katika kila kitu unachotaka kuitumia kulingana na maana yake, ambapo hata hivyo hii iliyotajwa ndio inayofaa Zaidi.' *(Imam Al Buhuti Sharh Muntaha Al Irada)*

Tunamalizia kwa kaauli ya Imam Shams Al Dīn Muḥammad Ibn 'Abd Al Raḥmān Al **Sakhāwī** Al Shafii ambae anasema kua: **'Kwa hakika Umma umekubaliana kua Istihadhah hua ni kusema**

أَعُوذُ بِاَللَّهِ مِنْ الشَّيْطَانِ الرَّجِيم

Audhu Bi Allahi mina Al Shaytani Al Rajiimi – Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Shaytani alielaaniwa.'(Jumaal Al Qurra)

Hivyo kama mtu anaingia kwenye Sala akisahau au kama ikiwa kwa makusudi hakua ni mwenye kuisoma Dua ya Istiftah na kisha akaanza moja kwa moja kusema *Audhu bi Allahi mina Al Shaytani Rajiimi*, basi kwa kua ameshafkia katika hatua hio basi hawezi kurudi nyuma tena katika Dua ya Ufunguzi, bali mtu huyo atatakiwa kuendelea kwa kuanza kuingia kwenye nguzo ya nne ya Sala ambayo na kusoma Surat Al Fatiha ambayo hua inaanza kwa*Tasmiyah* yaani kwa kusema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim.*

TASMIYAH - BIISMI ALLAHI RAHMANI RAHIM

❖❖❖

﴿بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ﴾

Tasmiya maana yake hua ni Kutaja Jina, Kutoa Jina au Kukipa Jina Kitu, Kumpa Mtu Jina au Cheo, Kuteua kitu fulani kwa ajili ya Jambo fulani, na hivyo neno hili hua pia linatumika kwa ajili ya kumaanisha neno *Bismi Allahi Rahmani Rahim.*

Na katika kuangalia Utamkwaji wa *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* katika Sala, basi tunaona kua kuna mitizamo tofauti juu yake kama ni miongoni mwa Aya za Qur'an ama la, ni aya ya mwanzoni mwa *Surat Al Fatiha* ama la na tofauti hii ndio iliyopelekea kutokea kwa utofauti wa mitizamo baina ya Wanazuoni kua ni wenye kuvutana kama inasomwa kabla ya *Surat Al Fatiha* ama la.

Na ingawa Wanazuoni wanakubaliana kua ni *Bismi Allahi Rahmani Rahim* ni sehemu yaaya *katika Surat An Naml* pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kukielezea kisa cha Nabii Sulaiman*Alayhi Salam* katika Barua aliyoiandika Nabii Sulaiman*Alayhi Salam*kumpelekea Balqis Malkia wa Sheba kama inavyosema aya:

﴿إِنَّهُ مِن سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُ بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ﴾

Innahu min sulaymana wa-innahu bismi Allahi alrrahmani alrraheemi*(Surat An Naml 27:30)*

Tafsir: ***Kwa Hakika Hii imetoka kwa Sulaiman na kwa Hakika imeanza kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwingi wa Huruma.***

Hivyo baadhi ya Wanazuoni wanasema kua: **'*Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni kiapo ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekitumia katika kila mwanzoni wa Sura , na hivyo kutokana nacho kiapo hicho basi amekua ni mwenye kusema kua: 'Hiki nilichokushushieni enye Waja wangu kwenye Sura hii ni cha Kweli, hivyo nitatekeleza kwa ajili yenu kila kitu nilichokisema nakukiahidi ndani yake Sura hii kwa ukarimu na huruma.''**

Ambapo anasema Abu Maljam kua: **‘Kuna mtu alikua anatembea juu ya kipando chake nyuma ya kiando cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kumwambia mtu huyoWakati mnyama wako atakapojikwaa basi usiseme kua Shaytan amemsababishia mnyama wangu kujikwaa, kwa sababu ukisema hivyo basi unamzidisha kichwa Shaytan na kua mkubwa kama nyumba huku akisema kwa ari: ‘Hakika nimeshafanikiwa’, hivyo sema badala yake: ‘Bismi Allahi Rahmani Rahiim’ na hivyo Shaytan atakua mdoogo kama Nzi.’***(Imam An Nasai)***

Ambapo anasema *Jarrah Allah Sultan Al Balagha* Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kua**: ‘Wanasema Wanazuoni wa Mji wa Madina, Mji wa Basra na Mji wa Sham kua *Tasmiyat* - *Bismi Allahi Rahmani Rahim*- Si miongoni mwa Aya za *Surat Al Fatiha.’***

Na Jarah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakhshari amesema hivyo kwa sababu amesema Imam Malik Ibn Anas ambae ni Muanzilishi wa Madhhab ya Imam Maliki kua: **'*Bismi Allahi* sio Aya kutoka katika Aya za Qur'an tukufu, isipokua ni sehemu ya Aya ya *Surat An Naml, Bismi AllahiRahmani Rahiim* iliandikwa mwanzoni mwa Sura kwa ajili ya kua ni Ufunguo tu wa Sura husika kwa ajili ya kupata Baraka zake na kwa ajili ya Kutengenisha baina ya mwanzo na mwisho wa Sura .'**

Na Mtizamo huu pia ni Mtizamo wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*, Al Qarri Abd Allah Ibn Mabaad, Imam Nuuman Ibn Thabit Abu Hanifa, Imam Al Awzai, n.k. Hivyo Mtizamo huu ndio mtizamo unaotegemewa na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik na kutumika katika Fiqh ya Ibada ya Sala katika Madhhab yao, ikiwemo pamoja na ule mtizamo wa kuachia mikono, *Ta’awudh* na *Tasmiyah* ni kua haipendekezwi katika Sala za Fardhi .

Kwani anasema *Mujaddid Ad Din* Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Tayyib Al Baqillani Al Basri Al Maliki kua: ‘**Sikupata Ushahidi Mimi ulio wazi wa Kauli wala maelezo yanayokubalika zaidi ya kushikamana na Hadith zinazothibitisha vyenginevyo. Katika Sahih Muslim kuna Hadith isemayo Aisha *Radhi Allahu Anha* amesema kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akianza Sala kwa kufanya Takbir na kisha kusoma *Alhamd lillahi Rabbi Al Alamiin.*Na Imam Muslim pia amesema kua**: **Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: Mimi nimesali Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhu* na Wote walikua wakianza na *Alhamd lillahi Rabbi Al Alaamiin,* hawakuwahi kusoma *Bismillahi Rahmani Rahiim* mwanzoni mwa Sala zao wala Mwishoni mwa Sala zao’**

Ambapo huo pia ndio mtizamo wa Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Al Qurtubi ambae anasema kua**: ‘Kuna Watu ambao wanasema kua *Bismi Allahi Rahmani Rahim*ni sehemu ya Qur'an, Imam Daraqutni ameelezea hayo, na sisi hatupingi hayo lakini sisi pia tunavithibitisho vinavyoonesha vyenginevyo kutoka kwa Maimam wetu na Wanafiqh wetu.'**

Hivyo Al Faqih Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Muhamad Ibn Rushd Al Qurtubi Al Maliki Al Andalus anaendelea kusema kua: ‘**Katika Sahih Muslim kuna Hadith isemayo Aisha *Radhi Allahu Anha* amesema kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akianza Sala kwa kufanya Takbir na kisha kusoma *Alhamd lillahi Rabbi Al Alamiin.*Na Imam Muslim pia amesema kua**: **Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: Mimi nimesali Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhu* na Wote walikua wakianza na *Alhamd lillahi Rabbi Al Alamiin,* hawakuwahi kusoma *Bismillahi Rahmani Rahiim* mwanzoni mwa Sala zao wala Mwishoni mwa Sala zao. Hivyo Madhhab yetu inapendelea hivyo na ndio Sahih kwa sababu ndani ya Masjid An Nabawi Madina imepita miaka mingi tangu wakati wa *Rasul***

Allah Salallahu Alayhi wa Salam **hadi wakati wa Imam Malik watu walikua wakifuata Sunnah na hakukua na mtu hata mmoja aliesema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim.'***

Kwani Hivyo Al Faqih Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Muhamad Ibn Rushd Al Qurtubi Al Maliki Al Andalus anamalizia kwa kusema kua: '**Lakini hata hivyo katika Madhhab yetu hua tunapendelea Kuitamka *Bismi Allahi Rahmani Rahim* katika Sala za Sunna, na kuna Hadith zinazothibitisha hivyo, na Imam Malik amesema Hakuna Makosa kuisoma *Bismillahi Rahmani Rahim* katika Sala za Sunna au katika kisomo cha Qur'an.'**

Hivyo Al Faqih Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Muhamad Ibn Rushd Al Qurtubi Al Maliki Al Andalus anaendelea kusema kua: '**Kuna Baadhi ya Watu wa Madina wanasema kua Ni lazima kuitamka *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* na miongoni mwao ni Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* na Imam (Muhammad Ibn Muslim Ibn Ubaydullah Ibn Abd Allah) Ibn Shihab Az Zuhri, Imam Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is'haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Thawr na Imam Abu Ubayd, hivyo hili ni jambo la Ijtihad na kimtizamo na wala si la kua ndio hukmu ya mwisho kama wanavyodhania baadhi ya Wajinga.'**

Kisha Hivyo Al Faqih Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Muhamad Ibn Rushd Al Qurtubi Al Maliki Al Andalus anasema kua: '**Na Ucha Mungu hua ni Kusoma *Bismi Allahi Rahmani Rahim* mwanzoni mwa Surat Al Fatiha, lakini si kwa Sauti bali kimoyomoyo.'***(Jamii Ahkami Al Qur'an)*

Ambapo tunapomkamata Mwanazuoni mahiri mwengine wa Madhhab ya Imam Malik ambae ni Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din Ibn Arabi basi tunaona kua yeye anasema kua: '***Surat Al Fatiha*** **inaitwa *Fatihat Al Kitab* na pia *Sabaa Al Mathani* na pia *Qur'an Al Adhiim* na pia *Ummu ul Quran*. Na pia *Ummu ul Kitab*na pia *Al Kifayat* na pia*Surat Al Hamd* na *Bismi Allahi Rahmani* Rahiim ni aya miongoni mwa aya zake. Na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim*inaitwa Ayat Al Mustaqila - Aya inyojitegemea - kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameijaalia kua ni yenye kuanzia katika kila Sura za Kitabu chake kitukufu cha Qur'an.'**

Shaykh Al Akbar Muhyi Ad Din Ibn Arabi ambae ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Maliki anamalizia kwa kusema: '**Kwangu mimi *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni aya katika aya za Qur'an kwani haiwezi kutoka ndani yakewakati ikiwa imerudiwa rudiwa katika kuzitenganisha Sura za Qur'an.'**

Hivyo huo ni mtizamo wa kwanza kuhusiana na Tasmiyah ambapo mtizamo wa pili ni wa Wanazuoni wasemao kua: **'*Tasmiya au Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni Aya ya Mwanzoni mwa Surat Al Fatiha tu.'**

Ambapomiongoni mwa wenye mtizamo pia ni huu ni Imam Mwanafiqh maaraufu wa Iraq mwenye asili ya Kiafrika ajulikanae kama Imam Said Ibn Jubayr kama alivyoelezea Imam Abd Razak katika *Musannaf* Ibn Abd Razzak, katika *Baab Qiraat Bismi Allahi Rahmani Rahiim.*

Na mtizamo huu pia umenukuliwa na wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Fiqh na Wanazuoni wa Usomaji wa Qur'an wa Tabiina.

Ambapo Mitizamo hii imenukuliwa na Imam Az Zuhri, Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Thawr, Imam Muhammad Kaab Al Qurazi.

Ambapo ukiangalia kwa umakini basi unaona kua wengi wa waliounukuu ni wanafunzi pia wa Imam Al Shafii, kama Imam Hanbal, Imam Is-haq, Imam Abu Thawr n.k na kwa upande wa Imam Al Shafii pia tunaona kua kuna mwalimu wake ambae ni Imam Al Zuhri, ila inabidi tufahamiane kua hawa wamemukuu tu kua kuna wenye Mitizamo pia kwani wao huu si Mtizamo wao kama tutakavyoona hapo baadae In-sha Allah.

Na tunapoangalia kuhusiana na Wanazuoni wanaoamini kua *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni aya ya Mwanzoni mwa Surat Al Fatiha tu, basi wao wanasimamia kwenyeVithibitisho vifuayavyo:

1-*Surat Al Fatiha* yenyewe Inaitwa *Sabaa Al Mathani* yaani Aya Saba zenye kurudiwa rudiwa, na ili uzipate Aya Saba hizo basi lazima na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* uijumlishe ndani yake, kwani vyenginevyo zitakua ni aya Sita tu.

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Hanifa basi yeye anasema kua: 'Aya ya *Saba ya Surat Al Fatiha ni Ghayri Al Maghdhuubi Alayhim wala Aldhdhaliin.'*

2- Ni kua Amesema *Umm Ul Muuminina* Salamah R*adhi Allahu Anha* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akiisoma Qur'an basi alikua akisitisha kisomo chake kila baada ya Aya, aya kwa aya Yaani *Bismi Allahi Rahmani Rahiim...Alhamd Lillahi Rabbi Al Alamiin...ArRahmani Rahiim..(Imam Abu Daud)*

Ambapo katika Hadith hii basi Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* alikua akifahamamisha namna *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyokua akisoma Surat Al Fatiha kua alikua akianza na Tasmiyah, na hivyo hii inamaanisha kua *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni Aya ya Mwanzo ya Surat Al Fatiha.

3- Hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambae aliulizwa kuhusiana na Kisomo cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Ambapo nae akajibu kwa kusema kua kilikua ni kizito cha kuvuta, na kisha Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*akaanza kusoma kwa kuvuta:*Bismi Allahi Rahmani Rahiim*.*(Imam Bukhari)* kama inavyosema hadith:

سأل أنس: كيف كانت قراءة النبي ﷺ فقال: كانت مدا، ثم قرأ: {بسم الله الرحمن الرحيم}، يمد ببسم الله، ويمد بالرحمن، ويمد بالرحيم.

Na hivyo Wanazuoni wanasema kua kama ingekua *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* si aya ya mwanzoni mwa *Surat Al Fatiha* basi *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*asingeisoma kwa uzito wake na kuivuta kama asomavyo Qur'ankwa usomaji wa kutiririka polepole, huku akichomoa herufi kutoka katika silabi zake, na kuvuta kile kinachostahiki kuvutwa kutokana na uasili ambao ni kutakiwa kua na ukamilisho wa herufi inayoifuata, alif, waw, au yaa, na kutovuta na herufi isiyo ya asili, ambayo hufuatwa na hamza, na imeunganishwa na kutengwa.

4- Hadith ya Nuaym Al Mujmar isemayo kua:

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَبْدِ الْحَكَمِ، عَنْ شُعَيْبٍ، حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، حَدَّثَنَا خَالِدٌ، عَنِ ابْنِ أَبِي هِلاَلٍ، عَنْ نُعَيْمٍ الْمُجْمِرِ، قَالَ صَلَّيْتُ وَرَاءَ أَبِي هُرَيْرَةَ فَقَرَأَ { بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ } الرَّحِيمِ ثُمَّ قَرَأَ بِأُمِّ

الْقُرْآنِ حَتَّى إِذَا بَلَغَ { غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلاَ الضَّالِّينَ } فَقَالَ آمِينَ . فَقَالَ النَّاسُ آمِينَ . وَيَقُولُ كُلَّمَا سَجَدَ اللَّهُ أَكْبَرُ وَإِذَا قَامَ مِنَ الْجُلُوسِ فِي الاِثْنَيْنِ قَالَ اللَّهُ أَكْبَرُ وَإِذَا سَلَّمَ قَالَ وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ إِنِّي لأَشْبَهُكُمْ صَلاَةً بِرَسُولِ اللَّهِ

Nilisali mimi nyuma ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu,* nae akasoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim,* na kisha akasoma *Ummu Al Kitab* hadi alipofikia kwenye maneno ya aya isemayo *Ghayri Al maghdhuubi AalayhimWala Dhaliiin,* nae akasema Amiiin, na watu wakaitikia Amiin. Na kila alipokua akisjudu alikua akisema Allahu Akbar! Na alipokua akitoka kwenye Sijda alisema Allahu Akbar! Na alipomaliza kutoa Salam basi alisema:Nnaapa mimi kwa yule ambae Roho yangu iko mikononi mwake kua Nimekufananishieni Sala yenu hii na Sala *ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'(Imam An Nasai)***

Ambapo hata hivyo hadithi hii ina sifa ya Udhaifu kulingana na mitizamo na vigezo vya baadhi ya Wanazuoni.Na tatizo ni kua hadith inaweza ikawa Dhaif kwa vigezo vya Imam mmoja ambapo nae akaikataa lakini ikawa inaaminika kwa vigezo vya mwengine na hivyo nae akaikubali.

5 - Na amesema tena Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ukisoma Surat Al Fatiha basi anza na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim,*kwani hio ni *Ummu ul Qur'an,Ummu Al Kitab, Sabaa Al Mathani na Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni moja kati ya Aya zake'*(Imam Ad Daraqutni, Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo anasema Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din Ibn Arabi ambae anatuambia kua: '**Unaposoma *Surat Al Fatiha* basi unaanza na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ambayo unatakiwa Uisome kwa kisomo cha pumzi moja bila ya kuikatisha.'**

Imam Abu Hanifa anasema kua: '**Tasmiyah ni aya ya Qur'an ambayo imeshushwa kwa ajili ya kutofautisha baina ya mwanzo na mwisho wa Sura tofauti, lakini hatahivyo Tasmiya hua si sehemu ya Sura husika isipokua ni aya ya Surat An Naml ambayo ndani yake imebeba maneno *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* hivyo *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* inatakiwa kusomwa katika Surat zote isipokua Surat At Tawba ambayo baada kuimaliza kuisoma Surat Al Anfal basi moja kwa moja unaingia kwenye Surat At Tawbah.'**

Na tunapoiangalia ayah ya mwanzo ya *Surat At Tawbah* ambayo inaanza na aya isemayo:

﴿ بَرَآءَةٌ مِّنَ ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦٓ إِلَى ٱلَّذِينَ عَاهَدْتُّمْ مِّنَ ٱلْمُشْرِكِينَ۞ فَسِيحُواْ فِى ٱلأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَٱعْلَمُوٓاْ أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِى ٱللَّهِ وَأَنَّ ٱللَّهَ مُخْزِىٱلْكَافِرِينَ﴾

Bar<u>a</u>atun mina All<u>a</u>hi warasoolihi il<u>a</u> all<u>adh</u>eena AA<u>a</u>hadtum mina *almushrikeena,*Fasee<u>h</u>oo fee Al ar<u>dh</u>i arbaAAata ashhurin waiAAlamoo annakum ghayru muAAjizee All<u>a</u>hi waanna All<u>a</u>ha mukhzee alk<u>a</u>fireena *(Surat At Tawbah 9:01-2)*

*Tafsir:**Uhuru wa kimajukumu (ya kaihadi) unatangaziwa kutoka kwa Allah (Subhanah wa Ta'ala)na Mtume wake (Salallahu Alayhi wa Salam) kwa hao ulio ahidiana nao(Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) miongoni mwa Washirikina. Hivyo Safirini (Enyi Washirikina) kwa miezi mine***

juu ya aradhi, lakini jueni kua kamwe hamtoweza Kuepuka Adhabu ya Allah, na Allah atawadhalilisha Makafiri.

Basi tunaona kua anasema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*kua**: 'Sura hii ambayo hua pia inajulikana kama Surat Baraat ina majina mengi ambapo miongoni mwao ni pamoja na 'Dharaulisho' kutokana na kua hii ni Sura yenye kuwajumuisha watu wa aina zote (Waumini, Makafiri, Wanafi, Wanaoishi Mijini, Mabedui, Mayahudi, Mapagani n.k) kua ni wenye kukatiwa na kushushwa darja zao, vyeo vyao, Mamlaka yao na kuwaonya kwa kuwadhihirishia udhaifu wao'**

Na Sura hii imeitwa Surat Baraat kwa sababu ya neno la mwanzo la aya ya mwanzo ya Sura h hii, na imeitwaSurat At Tawbah kwa sababu ndani yake katika aya ya 102 basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* anasema:

﴿وَمِمَّنْ حَوْلَكُمْ مِّنَ ٱلأَعْرَابِ مُنَافِقُونَ وَمِنْ أَهْلِ ٱلْمَدِينَةِ مَرَدُواْ عَلَى ٱلنِّفَاقِ لاَ تَعْلَمُهُمْ نَحْنُ نَعْلَمُهُمْ سَنُعَذِّبُهُم مَّرَّتَيْنِ ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَىٰ عَذَابٍ عَظِيمٍ۞وَآخَرُونَ ٱعْتَرَفُواْ بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُواْ عَمَلاً صَالِحاً وَآخَرَ سَيِّئاً عَسَى ٱللَّهُ أَن يَتُوبَ عَلَيْهِمْ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴾

Wamimman hawlakum mina Al aAArabi munafiqoona wamin ahli almadeenati maradoo AAala alnnifaqi la taAAlamuhum nahnu naAAlamuhum sanuAAadhdhibuhum marratayni thumma yuraddoona ila AAadhabin AAa*dh*eemin ;Waakharoona iAAtarafoo bidhunoobihim khalatoo AAamalan salihan waakhara sayyi-an AAasa Allahu an yatooba AAalayhim inna Allaha ghafoorun raheemun*(Surat At Tawbah 9:102)*

Tafsir: **Na Miongoni mwa Mabedui wanaokuzunguka, baadhi yao ni Wanafiq. Na pia baadhi ya watu wa Madina, wanazidi na kudumu kwenye Unafik, Ila wewe (Muhammad) huwajui, sisi tunawajua. Na ttawaadhibu mara mbili zaidi na Akhera watapelekwa kwenye Adhabu kubwa sana; Na pia kuna wengine wanaozijua na kuzikubali Dhambi zao, kwani wamechanganya Amali njema pamoja na amali mbovu, Labda Allah atawageukia kwa usamehevu, kwani kwa hakika Allah ni mwingi wa usamehevu na ni mwingi wa Huruma.**

Na pia akasema katika ya 117 hadi 118 kua:

﴿لَقَدْ تَابَ اللهُ عَلَىٰ ٱلنَّبِيِّ وَٱلْمُهَاجِرِينَ وَٱلأَنصَارِ ٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ ٱلْعُسْرَةِ مِن بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيغُ قُلُوبُ فَرِيقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ إِنَّهُ بِهِمْ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ۞وَعَلَى ٱلثَّلاَثَةِ ٱلَّذِينَ خُلِّفُواْ حَتَّىٰ إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ ٱلأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ أَنفُسُهُمْ وَظَنُّوۤاْ أَن لاَّ مَلْجَأَ مِنَ ٱللَّهِ إِلاَّ إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوۤاْ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ﴾

Laqad taba Allahu AAala alnnabiyyi waalmuhajireena waAl ansari alladheena ittabaAAoohu fee saAAati alAAusrati min baAAdi ma kada yazeeghu quloobu fareeqin minhum thumma taba AAalayhim innahu bihim raoofun raheemun; WaAAala alththalathati alladheena khullifoo hatta idhadhaqat AAalayhimu Al ardhu bima rahubat wadhaqat AAalayhim anfusuhum wa*dh*annoo

an la maljaa mina Allahi illa ilayhi thumma taba AAalayhim liyatooboo inna Allaha huwa alttawwabu alrraheemu.*(Surat At Tawbah 9:117-118)*

Tafsir: ***Allah (Subhanah wa Ta'ala) amemsamehe Mtume(SalallahuU Alayhi wa Salam), Muhajirina (Waliofanya Hijra kwa kuhamia Madina) na Ansari (Na Watu wa Madina waliowanusuru wahamiaji hao) wlaiomfuata Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam katika wakati wa matatizoya Msafara (wa Tabuk) baada ya Nyoyo za baadhi yao zikaribie kupotoka, lakini amekubalia Toba zao. Kwa hakika yeye ni mwenye kua na huruma juu yao na mwingi wa Rehma kwao. Na amewasamehe pia watatu walioachwa (ambao hawakujumuika katika Matatizo ya Msafara wa Tabuk) wabakie ardhini kwani ardhi ni pana ingawa ilikua imebanwa na nafsi zao zimebanwa kwa ajili yao, na wakaona kua hakuna kukimbia kutoka kwa Allah(Subahanh wa Ta'ala)na hakuna kwa kukimbilia isipokua kwake. Hivyo amekubali Toba ili waweze kutubu kwake. Kwa haikia Allah Subhanah wa Ta'ala ni mwenye kukubali Toba na ni mwingi wa Rehma.***

Ambapo wanasema *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakalimin* Imam Fakhr Ad Din Al Razi, Jarrah Allah Sultan Al Balagha Imam Abu Qasim Al Zamakhshari, na Imam Al Qurtubi wanasema kua: **'Hii ndio Sura ya Mwisho kushushwa ingawa ndani yake haijabeba aya ya mwisho kushushwa.'**

Na amesema Baraa Ibn Adhib Al Ansari *Radhi Allahu Anhu*kua: **'Aya ya mwisho kushushwa ni ile isemayo kua'**

﴿يَسْتَفْتُونَكَ قُلِ ٱللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِى ٱلْكَلَٰلَةِ إِنِ ٱمْرُؤٌا۟ هَلَكَ لَيْسَ لَهُۥ وَلَدٌ وَلَهُۥٓ أُخْتٌ فَلَهَا نِصْفُ مَا تَرَكَ وَهُوَ يَرِثُهَآ إِن لَّمْ يَكُن لَّهَا وَلَدٌ فَإِن كَانَتَا ٱثْنَتَيْنِ فَلَهُمَا ٱلثُّلُثَانِ مِمَّا تَرَكَ وَإِن كَانُوٓا۟ إِخْوَةً رِّجَالًا وَنِسَآءً فَلِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ ٱلْأُنثَيَيْنِ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمْ أَن تَضِلُّوا۟ وَٱللَّهُ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمٌ﴾

Yastaftoonaka quli Allahu yufteekum fee alkalalati ini imruon halaka laysa lahu waladun walahu okhtun falaha nisfu ma taraka wahuwa yarithuha in lam yakun laha waladun fa-in kanata ithnatayni falahuma alththuluthani mimma taraka wa-in kanoo ikhwatan rijalan wanisaan falildhdhakari mithlu ha*dhdh*i Al unthayayni yubayyinu Allahu lakum an tadilloo waAllahu bikulli shay-in AAaleemun*.*(Surat Al An Nisaa 4:176)*

Tafsir: ***Wanakuuliza kuhusiana na hukmu ya kisharia, waambie kua: 'Allah anaelekeza kuhusiana na Kalalah (wale Waislam wanaokufa ila ya kuwacha watoto wa kurithi), kua kama mtu akifa akiwa amewacha Dada lakini hakua na mtoto basi Dada atapata nusu ya Mirathi, na kama aliefariki ni Mwanamke(na hakuacha mtoto)basi Kaka yake atapata urithi wake. Na kama kuna Dada wawili basi watachukua sehemu mbili kati ya tatu ya mirathi na kama ikiwa kuna Kaka na Dada basi Kaka atapata mara mbili zaidi ya Dada. Hivyo ndivyo ambayo Allah(Subhanah wa Ta'ala) anaweka wazi juu yenu ili msipotoke, na Allah ni mwenye kujua juu ya kila kitu.'***

Hivyo Surat At Tawbah ndio Sura ya mwisho kushushwa mbali ya kua hakuna aya ya mwisho kushushwa ndani yake, na anasema Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi kua**: 'Surat At Tawbah haina *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kwa sababu *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* mwenyewe hakua ni mwene kuisema mwanzoni mwa Sura h hii. Na hivyo Masahaba *Radhi Allahu Anhum*hawakuiweka pia na wala waliowafuatia baada yao, na huu ni uthibitisho wa ukweli wa kuakatika kuihifadhi Qur'an basi zilichukuliwa tahadhari na umakini mkubwa sana ili Qur'an ibakie katika hali yake ya asili.'**

Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi anaendelea kusema kua: **'Amesema Imam At Tirmidhii kua: 'Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alimuuliza: Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu,:* 'Hivi Kwanini *Surat Al Anfal* imewekwa miongoi mwa Sura ndefu wakati hii ni Sura fupi? Na kwanini Bismi *Allahi Rahmani Rahiim* haijawekwa kwenye Surat At Tawbah?'**

Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Wakati Sura na Aya zilipokua zikishushwa, ilikua ni kawaida ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kuamrisha ziandikwe huku akiwa ni mwenye kudhihirisha aya gani ikae katika sehemu gani. *Surat Al Anfal* ilikua ndio Sura ya Mwanzo kushushwa katika Mji wa Madina na *Surat At Tawbah* ndio Sura ya mwisho kushushwa katika Mji wa Madina, na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakua na nafasi ya kusema wapi iwekwe Surat At Tawbah, na ukiziangalia kwa mtizamo wa mada zake basi ni zenye kufanana, hivyo mimi nikaziweka pamoja bila ya kuweka *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* baina yake na hivyo kuziweka Sura mbili hizi baina ya Sura ndefu.'''

Ambapo anasema Hivyo Al Faqih Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Muhamad Ibn Rushd Al Qurtubi Al Maliki Al Andalus kua: **'Kuna sababu kadhaa ambazo zinaelezea kwa nini Bismi Allahi ikawa ni yenye kuachiwa kwenye Surat At Tawbah, ambapo moja wapo kati yao ni kua:'Surat At Tawbah imeanzia na vitisho wakati *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni maneno yenye kuahidi Rehma na Huruma. ''**

Ambapo anasema Imam Malik Ibn Anas katika Malik Muwatta kua: '**Surat At Tawbah ilikua ni miongoni mwa Sura ndefu kama Surat Al Baqara, lakini Allah Subhanah wa Ta'ala akamjaalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua n mwenye kuisahau sehemu ya mwanzoni mwa Sura hio na hivyo *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ikawa ni miongoni mwa aya zilizosahauliwa na Sura hio'**

Ambapo Imam Al Jazari na Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Musa Al Shatibi Al Andalus Al Malikibasi wao wanasema kua: **'Mtu anapomaliza kusoma Surat Al Anfal na akataka kuingia kwenye Surat At Tawbah basi hatakiwi kusoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* lakini anaweza kusema *Audhu Bi Allahi mina al Shaytan Rajiimi'* kwa maana hio basi Mtu anaruhusika kusoma B*ismi Allahi* kama atasoma popote pale ndani ya Qur'an isipokua katika aya ya mwanzo ya *Surat At Tawbah,* na hivyo kwa mfano kama ataianza Surat At Tawba kuanzia katika aya za mbeleni basi anaweza kusoma *Bisimi Allahi Rahmani Rahiim.***

Na anasema Imam Abu Hanifa kua: **'Tasmiya - *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni aya ambayo imeshushushwa kwa ajili ya kutofautisha baina ya Mwanzo na Mwisho wa Sura za Qur'anAmbapo hata hivyo *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* hua si sehemu ya Sura husika, isipokua katika Surat An Naml, ambayo ndani yake imebeba maneno *Bismi Allahi Rahmani Rahiim.'***

Kwa maana hio basi Imam Abu Hanifa na baadhi ya Wanazuoni wengineo akiwemo Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Al Awzai, Imam Al Hakam, Imam Hammad Ibn Salamah n.kBasi wao wanasema kua:**'Ndio *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* inatamkwa kabla ya Kuisoma Surat Al Fatiha ndani ya Sala, lakini hua haitamkwi kwa Sauti, bali hua inatamkwa kimya kimya'**

Ambapo Mtizamo huu ni wenye kutokana na Hadith ya Anas Ibn Malik*Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema:'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha sisi na hatukumsikia akisema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim.'(Sahih Muslim)***

Ambapo anasema Imam Ibn Daqaiq Al Idd kua; **'Hadithi hii ndio inayotumiwa kua kama uthibitisho wa wale wasiosoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kwa sauti mwanzon mwa Sala, kwani Wanazuoni wana mitizamo mitatu juu ya jambo hili, ambapo wa kwanza ni kua *Bismi Allahi Rahmani Rahim* hasomwi kwa Sauti wala kimya kimya ambao ni Mtizamo wa Imam Malik, na mtizamo wa pili , kua *Bismi Allahi Rahmani Rahim* hasomwi kwa Sauti bali kimya kimya ambao ni Mtizamo wa Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad Ibn Hanbal, na wa tatu ni kua *Bismi Allahi Rahmani Rahim* husomwa kwa Sauti katika Sala za Sauti na husomwa kimya kimya katika Sala za Kimya ambao ni Mtizamo wa Imam Al Shafii.'** *(Ihkamu Al Ahkam Sharh Umdat Al Ahkam)*

Na ukweli ni kua tunapowaangalia wengi kati ya Wanazuoni wenye Mtizamo huu basi tunaona kua ni Wanazuoni wenye Asili ya Iraq.Kama vile ambavyo ilivyokua mtizamo wa mwanzo wa kua *Bismi Allahi* haifai au haina ulazima kuisoma kwenye Sala kabla ya Surat Al Fatiha katika Sala ya Fardhi kua ni wenye kubebwa na Wanazuoni wengi wa Mji wa Madina yaani kina Imam Malik.

Na hivyo tunapoangalia mtizamo huu wa pili ambao asili yake ni Iraq basi haishangazi sana kuona kua Imam Abu Hanifa, na wengineo wa Iraq wameubeba mtizamo huu, na hii ni kwa sababu Ngao ya Ilm ya Fiqh ya Ardhi ya Iraq yakiwemo Madhhab ya Imam Abu Hanifa inabebwa na Sahaba mwanazuoni aitwae Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu.* Na Maimam wote tuliowataja wanaofuata Msimamo huu ni watu wa Iraq, hata Imam Ahmad Ibn Hanbal mwenyewe.

Na hata Imam Al Shafii aliishi nchini Iraq na akamsomesha Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Al Shafii alipohama Iraq basi alisema: **'Sikuacha mimi mtu mwenye Ilm katika Ardhi ya Iraq kama Ahmad Ibn Hanbal'**

Kwani kwa upande mwengine basi Fiqh ya Iraq imebeba pia mitizamo ya *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambae nae aliwahi kua Gavana wa Iraq, na hata alienukuu Hadith hii ambae ni Sahaba Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*aliishi na Kufariki katika Mji wa Basra nchini Iraq.

Hivyo bila ya shaka hili la kua na mtizamo huu kwa wengi miogoni mwa Wanazuoni wa Iraq na waliosoma Iraq hua halishangazi sana kwani Miongoni mwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wenye mtizamo huu mbali ya Anas Ibn Malik, lakini pia mtizamo huu ni wa Abd Allah Ibn Masud, Ali Ibn Abi Talib, Abd Allah Ibn Zubayr na Amar *Radhi Allahu Anhum* ambapo takriban wote hawa ndio wanajumuisha asili ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Na wote hawa wanasimamia kwenye *asbab Nuzul* au Sababu ya kushushwa aya ya 110 ya Surat Al Israa ambayo wanasema kuhusiana nayo Imam Ad Dahaq, Imam Said Ibn Jubayr kua**: 'Makafiri walikuja msikitini na wakamkuta *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anasali akiwa anasema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim'***

Hivyo Makafiri hao wakasema: 'Ah! Mbona Huyu Muhammad anamtaja Rahman wa Mji wa Yamamah?'

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamuamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aitamke *Bismi Allahi Rahmani Rahim* kwa kimya kimya, baada ya kushusha maneno ya Surat Al Isra ya aya isemayo:

﴿قُلِ ٱدْعُواْ ٱللَّهَ أَوِ ٱدْعُواْ ٱلرَّحْمَٰنَ أَيّاً مَّا تَدْعُواْ فَلَهُ ٱلأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ وَلاَ تَجْهَرْ بِصَلاَتِكَ وَلاَ تُخَافِتْ بِهَا وَٱبْتَغِ بَيْنَ ذَٰلِكَ سَبِيلاً﴾

Quli odAAoo Allaha awi odAAoo alrrahmana ayyan ma tadAAoo falahu Al asmao alhusna wala tajhar bisalatika wala tukhafit biha waibtaghi bayna dhalika sabeelan*(Surat Al Isra 17:110)*

Tafsir:***Sema (Ewe Muhammad); 'Muombeni Allah au Muombeni Rahmani, kwa jina lolote lile mtakalomuombea (hua ni sawa tu) kwani kwake yeye ndio kwenye Majina Martukufu Na wala Usikuze Sauti katika Maombi yakoWala Usiombe kwa sauti ya chini bali Kua ni Mwenye Kutafuta njia baina ya hali hizo.***

Na anasema Imam Al Hakim Al Tirmidhii kua: '**Amrisho la aya hii limekua Likiendelezwa mbali ya kua Sababu iliyosababisha kutokea kwake haipo tena na hivyo *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* haitamkwi kwa sauti katika Sala za Sauti wala katika Sala za kimya'**

Kwani Mtizamo anaouzungumzia Imam Al Hakim Al Tirmidhi ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.Na hii ni kwa sababu kwa kua kwao wao *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* si sehemu ya Surat Al Fatiha bali ni Ufunguzi tu basi hua ni Sunnah kuisoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kimya kimya kwa Imam na kwa Maamuma iwe katika Sala ya Kutoa Sauti ama Sala ya Kimya Kimya.

Na hivyo Shaykh Muhammad Al Amin Ibn Muhammad Al Mukhtar Ibn Abd Al Qadir Al Jaknii Ash Shanqeeti anasema kua: '**Wanazuoni wametofautiana juu juu ya *Bismi Allahi* kua ni aya mwanzoni mwa kila Sura au ni aya mwanzoni wa *Surat Al Fatiha* tu au ni aya kamili inayojitegemea kama aya nyengine ama la.**

Ama kulingana na aya isemayo:

﴿إِنَّهُۥ مِن سُلَيْمَانَ وَإِنَّهُۥ بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ﴾

Innahu min Sulaymana wa-innahu bismi Allahi alrrahmani alrraheemi.

*Tafsir: **Hii ni kutoka kwa Sulayman na hakika inasema Biismi Allahi Rahmani Rahim** (Surat An Naml 27:30)*

Basi bila ya shaka hii ni moja kati ya aya za Qur'an na hii ni kulingana na makubaliano ya *Ijmaa.* Ama kuhusiana na *Surat Baraat (At Tawbah*) Basi *Biismi Allahi* sio miongoni mwa aya za Sura hio, lakini kuna kutofautiana kuhusiana na hayo mambo mengine, kwani baadhi ya Wanazuoni wa *Usul wamesema kua Biismi Allahi si miongoni mwa Aya za Qur'an* na baadhi wamesema kua ni miongoni mwa *Aya ya Surat Al Fatiha tu.* Na pia wako wanaosema kua *Biismi Allahi* ni Aya Mwanzoni mwa kila Sura , na huu ni Mtizamo wa *Imam Muhammad Idris Al Shafii*.

Na kulingana na Kauli zinazoaminika na kua na nguvu zaid katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa, ambazo ni zenye kutoka kwa Imam Abu Hanifa, Imam Abu Yusuf, Imam Ash Shaybani na Imam Ibn Al Hasan basi tunaona kua kuna mitizamo ifuatayo ambayo imenukuliwa katika vitabu tofauti, ambapo anasema Imam Aladiin Ibn Al Haskafi Al Hanafi kua:

'Ni Sunna iliyothibitishwa kusema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kimya kimya kabla ya Kusoma Surat A Fatiha katika kila Rakaa ya Sala.Na si Sunna iliyothibitishwa lakini hua haikirihishi kusema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* baina ya Kisomo cha Surat Al Fatiha na Sura nyengine katika Sala'

Na anasema *Khatima Al* Muhaqqiqin (ambae ni Muhakiki wa mwisho wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa) *Sayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafi.*

Naam, huyo ndio Imam Ibn Abidin Ash Shami Al Hanafi ambae ni mwyenye kutoka katika ukoo wa Kisharifu, na mbali ya kua na Ilm kubwa lakini pia alikua Maa-Shaa Allah, Amejaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* muonekano wa Mwili mzuri wenye Afya na uliopanda juu na kifua kipana na pia muonekano wa Uso wenye Sura yenye kuvutia sana.

Ambapo Imam Ibn Aabidin mwanzo alikua ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii lakini baadae akahamia kwenye Madhhab ya imam Abu Hanifa.Hivyo anasema Imam Ibn Abidin katika kufafanua Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua:**'Kama mtu akisoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* baina ya Surat Al Fatiha na Sura nyengine ndani ya Sala basi hivyo hua ni bora zaidi lakini kama ikiwa ataanza mwanzoni mwa Sura anayoisoma'***(Radd Al Mukhtar)*

Na anasema Imam Abu Ikhlas Ali Al Shurunbulali Al Hanafi kua; **'Kwa kua *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* si Wajib bali ni Sunna iliyothibitishwa basi mtu anapoisahau hua haimlazimikii Kuleta Sijdat As Sahw ambayo huhitajika kuifanya utakapoacha Nguzo ya Sala'***(Maraqi Al Falah)*

Ama kwa upande wa Aya hii ya *Surat Al Isra 17:110 isemayo:*

﴿قُلِ ٱدْعُواْ ٱللَّهَ أَوِ ٱدْعُواْ ٱلرَّحْمَٰنَ أَيّاً مَّا تَدْعُواْ فَلَهُ ٱلأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ وَلاَ تَجْهَرْ بِصَلاَتِكَ وَلاَ تُخَافِتْ بِهَا وَٱبْتَغِ بَيْنَ ذٰلِكَ سَبِيلاً﴾

Quli odAAoo Allaha awi odAAoo alrrahmana ayyan ma tadAAoo falahu Al asmao alhusna wala tajhar bisalatika wala tukhafit biha waibtaghi bayna dhalika sabeelan*(Surat Al Isra 17:110)*

*Tafsir: **Sema (Ewe Muhammad); 'Muombeni Allah au Muombeni Rahmani, kwa jina lolote lile mtakalomuombea (hua ni sawa tu) kwani kwake yeye ndio kwenye Majina Martukufu Na wala Usikuze Sauti katika Maombi yako Wala Usiombe kwa sauti ya chini bali Kua ni Mwenye Kutafuta njia baina ya hali hizo.***

*B*asi anasema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: **'*Rasul Allah Salallah Alayhi waSalam* alikua akimuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Jina la Ya Rahman, hivyo Mapagani wakasema kua anamuomba mtu aitwae Rahman *(Musalima Al kadhdhab)* anaeishi katika ardhi ya Yamamah.'**

Na kabla ya kuendelea mbele zaidi basi kwanzainabidi tuangalie kuhusiana na Idadi ya Aya za Surat Al Fatiha, kwani Ingawa Wanazuoni wanasema kua ni aya 7 ukijumuisha na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim*, lakini kuna watu ambao wanaweza wakajiuliza, Hivi Jee hawa wanaosema kua *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* sio sehemu ya Aya ya Surat Al Fatiha bali ni Ufunguo tu wa kila Sura, basi hua wanahesabu Surat Al Fatiha ina aya ngapi?

Na kuhusiana na suali hili basi anasema *Mujaddid Ad Din Imam* Abu Fadhl Abd Rahman Ibn Abu Bakr Ibn Muhammad Jalal Ad Din Al Suyyuti kuhusiana na Suali hili kua:**'Kulingana na Usomaji basi tunaona kua ziko aya 7 Lakini sasa Wanazuoni wa Mji wa Kufah na Makkah, hawakuijumuisha**

Bismi Allahi Rahmani Rahiim Na hivyo Wanasema kua maneno yasemauo An-aAamta Aalayhim ni aya inayojietegemea Ambapo kwa upande wa Wanaoihesabu Bismi Allahi Rahmani Rahiim basi wao wamefafanua kinyume chake yaani Sirata Al Ladhiina An-aAamta Aalyhim ni aya moja.

Na kwa upande mwengine basi Anasema Al Hasan Al Basr kua: Aya za Surat Al Fatiha ziko Nane, na kuna wanaosema kua ziko Sita na pia kuna wanaosema kua ziko aya Tisa Pale utakapokua unahesabu manenno *Iyyaka NaAabudu* kua ni aya moja na maneno *Waiyyaka NastaAin* kua ni aya nyengine.

Ambapo amir ul Muuminin Ali Ibn Abu Talib *Radhi Allahu Anhu* aliulizwa kuhusiana na Sabaa Al Mathani nae akajibu kwa kuanza kusoma: *Alhamd lillahi Rabbii Al Alaamiin.* Hivyo alipomaliza akaambiwa kua Ulizozisoma ni aya Sita tu.

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akasema pamoja na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim*(*Al Itqan fii Ulum ul Qur'an)*

Naam kwa maana hio basi ingawa Aya za Surat Al Fatiha ziko Saba na huu ndio mtizamo unaokubalika, lakini sasa hua kuna tofauti ya idadi kulingana na Kisomo cha Mwanazuoni husika kunakotegemeana na wapi anaposimama katika aya,yaani akiigawa aya mara mbili kulingana na kisomo na maana ya Aya basi kwake yeye idadi itabadilika.Na kutokana na hili basi ndio maana ikawa pia kuna utofauti wa Idadi ya Aya za Qur'an kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni kwani:

Kuna mtizamo usemao kua ziko Aya 6666 na hii ni kulingana na Mtizamo wa Aisha *Radhi Allahu Anha.*

Kuna mtizamo usemao kua ni aya 6239 ambao ni Mtizamo wa watu wa Mji wa Kufah unaotokana na *Amir ul Muumimnin* Ali Ibn Abit Talib *Radhi Allahu Anhu.*

Kuna mtizamo wa Wanazuoni wa Makka ambao ni kua: Ziko aya 6219.

Kuna mtizamo wa Wanazuoni wa Madina ambao ni kua Aya 6211.

Na kuna Mtizamo wa kua ni Aya 6236 bila ya kujumuisha na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* na ukijumuisha na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* basi inakua ni aya 6348.

Hivyo Qur'an ni ile ile ila aya hubadilika idadi kulingana na Wasomaji na usomaji wao kwa mfano Ayat Al Kursiy ni Aya moja tu, lakini ndani yake mna sentensi 9, na hivyo inakua vigumu kuisoma kwa Pumzi moja na hivyo inabidi usimame. Katika vituo visivyozidi Tisa ndani yake, ingawa pia unaweza kusimama mara mbili au tatu kulingana na pumzi zako na usomaji wako.

Hivyo katika Qur'an kuna aya ambazo ni ndefu sana na baadhi ya Wanazuoni wa Ilm ya Qiraa yaani ya Usomaji wa Qur'an basi wamezigawa baadhi ya aya hizo mara mbili kulingana na aina ya visomo vyao, au aya fupi lakini wakaigawa mara mbili kutokana na maana ya maneno ya Aya kwa mfano hii *Iyyaka Naabudu* - Ni wewe tu ndie tunaekuabudu, *wa Iyyaka nastaAiin* - Na ni wewe tu ndie tunaekutegemea katika msaada. Kua ni aya mbili kwa baadhi na kua ni aya moja kwa baadhi. Nadhani japo kidogo itakua tumefahamiana kwanini ikawa kuna mitizamo tofuati juu yake.

Na tunapoangalia katika sharia za Sharia za Dini ya Kiislam basi tunaona kua zinahimiza kumtaja*Allah Subhanah wa Ta'ala katika* kila kitendo cha Amali njema kama kula, kunywa, kuchinja, kungiliana kimwili, kujitoharisha, kupanda vyombo vya usafiri n.k kama zinavyothibtisha Aya pale ziliposema:

﴿ فَكُلُواْ مِمَّا ذُكِرَ ٱسْمُ ٱللَّهِ عَلَيْهِ إِن كُنتُمْ بِآيَاتِهِ مُؤْمِنِينَ ﴾

Fakuloo mimmadhukira ismu Allahi AAalayhi in kuntum bi-ayatihi mu/mineena*(Surat Al AnaAm 6:118)*

Tafsir: ***Hivyo kuleni kile kilichotajiwa Jina la Allah kama kweli nyinyi ni wenye kuamin Aya zetu.***

Na pia pale ziliposema aya kua:

﴿ وَقَالَ ٱرْكَبُواْ فِيهَا بِسْمِ ٱللَّهِ مَجْرَاهَا وَمُرْسَاهَا إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴾

Waqala irkaboo feeha bismi Allahi majraha wamursaha inna rabbee laghafoorun raheemun*(Surat Hud 11:41)*

Tafsir: ***Naakasema: 'Pandeni ndani yake kwa Jina la Allah iwe Safari yake na kuwasili kwake ardhini, kwani kwa hakika Mola wangu nimwingi wa Rehma n ni mwingi wa Huruma.'***

Na bila ya shaka *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliamrisha kwa kusema kama alivyosema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* katika hadith ifuatayo: **'*Amesema Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua: 'Wakati yanapotanda mabawa wa Usiku, basi wawekeni watoto wenu ndani, kwani Shaytani hua anatoka nje katika wakati huo, na kisha inapopita sehemu ya wakati wa Usiku basi waachieni na Fungeni Milango yenu na Tajeni Jina la Allah kwani Shaytani hafungui mlango uliofungwa kwa kutajiwa jina la Allah, Zimeni taa na tajeni Jina la Allah, fungeni vibuyu nyenu vya maji na tajeni Jina la Allah, funikeni vyombo vyenu na tajeni jina la Allah,Hata kama kwa kuwekea kitu juu yake na zimeni taa zenu**.*(Bukhari na Muslim)*

Ama kwa upande wa Imam Nasir Ad Din Al Baydawi anasema kua: '**Muongozo huu wa kuanza na kila kitu na *Biismi Allahi* unamfunzaMuumini kutafuta Baraka kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kila jambo lake katika maisha yake.**' *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Al Mushakiqin Shaykh ul Islami Imam Al Ghazali Al Thani Imam* Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na ayah hii kua: '***Biismi Allahi* hua inamfunza Muislam kuomba msaada kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia katika Neema na Baraka zake katika kila kitu chake na hivyo hua ni yenye kumfanya Muislam kuanza kila kitu chake na *Dhikr Allah*. Na ndio maana katika kufanya kila kitu chako basi kuisoma ayah hii hua inapendekezwa na hua na hali ya *Mandub* katika Sharia za Fiqh'**

Katika kufafanua zaid maana aliyoinisha *Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Al Muashakiqin Shaykh ul Islami Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi* katika kuielezea hali ya *Bismi Allah* kulingana na Sharia za *Fiqh* na matumizi yake basi tunaona kua:

1) ***Bismi Allah* hua ni *Fardhi* :** kuitamka pale Muislam anapotaka kuchinja mnyama kwa ajili ya kula au anaporusha Upinde, Mshale, Risasi wakati wa kuwinda au anapomuachia Mnyama wa kuwindia katika wakati wa kuwinda.

Na pia ni *Fardhi* kwa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii kuisoma katika Sala unaposoma *Surat Al Fatiha* au Mwanzoni mwa Sura nyengine yeyote isipokua *Surat At Tawba* ile kwa sababu *Bismi Allah* hua ni Moja kati ya aya ya mwanzo katika kila Sura isipokua *Surat At Tawba.* Na kuisoma kwa *Biismi Allahi* kwa Sala za Kutoa Sauti hua niWajib kwa kila Sura isipokua*Surat At Tawba* au unapoanza katikati ya Sura . Kusoma *Biismi Allahi* kwa Sauti hua kunaulainisha Moyo wa Msomaji.

Kwani anasema Imam Abu Zakariyyah Sharaf An Nawawi kua: '**Mtu anaetaka kusoma basi asome *Bismi Allah Rahmani Rahim* mwanzoni mwa kila Sura isipokua *Surat Baraa'ah (At Tawba),* kwa sababu wengi miongoni mwa Wanazuoni wamesema kua hii ni aya popote pale itakapoandikwa ndani ya *Mus-haf*.**

Na imeandikwa mwanzoni mwa kila Sura isipokua katika *Surat At Tawbah*. Hivyo kama atasoma mwanzoni mwa kila Sura isipokua *Surat At Tawba* basi hua na uhakika kua amesoma *Qur'an* nzima au Sura nzima. Na kama atakua hakusoma *Bismi Allah* basi atakua ameiacha sehemu ya *Qur'a*n na hii ni kutokana na mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni'

2) ***Bismi Allah* hua ni *Sunnah*** kuitamka wakati wa kusoma *Surat Al Fatiha* katika Sala kulingana na mtizamo wa Madhab ya Hanafi ambao ni mtizamo wa Imam Abu Hanifa, Imam Ibn Al Hammam na Imam Al Halabi.

3) ***Bismi Allah* hua si *Mustahab* wala si *Sunnah* na wala si *Makruh***kuitamka katika wakati wa kusoma *Surat Al Fatiha* katika Sala kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Yusuf.

4) Bismi Allah* hua ni *Makruh kuitamka katika wakati kuisoma *Surat At Tawba* ambayo haina *Biismi Allahi* mwanzoni mwake, ila kwa Mtizamo wa Imam Al Ramli basi hua ni Sunnah kuitamka unapoanza kati kati ya Sura hio ama kwa upande wa Imam Ibn Hajar Al Asqalani basi hua ni Sunnah kuisoma mwanzoni mwa *Surat Tawbah* na ni *Makruh* kuisoma wakati unapoanza kati kati ya *Surat At Tawba*.

Na pia hua ni *Makruh* kuitamka katika wakati wa kufanya mambo ambayo yana shaka ndani yake kwa mfano kama kuvuta sigara.

5) ***Bismi Allah* hua ni Mubah** kuitamka wakati wa kuanza kutembea, kukaa kitako au kusimama.

6) ***Bismi Allah* hua ni Haram** Kuitamka katika wakati wa kufanya mambo ya Haram, Kuitamka wakati unapokua na Janaba, Unapokua na Hedhi au Nifasi pale unapokua na nia ya kuisoma aya za Qur'an isipokua haiwi haram pale inapokua unafanya hivyo kwa sababu ya kutabarruk au kwa ajili ya kufanya Dhikr.

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '***Bismi Allahi Rahmani Rahim* ni moja kati ya Majina ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo baina yake na baina *ya Ismi Allahi Al Aadhiim* hua ni kama baina ya Weupe na Weusi wa Mboni ya Jicho Unalotumia kuangalia.'***(Imam Al Hakim, Imam Adh Dhahabi)*

Na akasema Bahr Al Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:***'Bismi Allahi Rahmani Rahim*** **imejaaliwa kwa Ummah wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tu, haikujaaliwa kwa Ummah mwengine wowote kabla yake.'**

Hapo kabla katika kungalia mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa tulimzungumzia Na anasema Khatima Al Muhaqqiqin (ambae ni Muhakiki wa mwisho wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa) Sayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafi.

Nimemrudia tena Al Aalamah, Al Muhaqqiqin Imam Ibn Aabidin, kwa sababu nataka kuangalia kuhusiana na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kwa upande wa Sala ya Madhhab ya Imam Al Shafii.Na hivyo basi kwa upande huu nataka tumkamate moja kwa moja Al Muhaqqiq wa Madhhab ya Imam Al

Shafii ambae yuko Juu zaidi Kiilm kwani yeye amefikia Darja ya Mujtajid Imam, na huyu si mwengine bali ni *Mujtahid Imam, Shaykh Ul Islami, Al Allamah, Al Faqih, Imam Al Muhaqqiqin Al Hafidh Imam Shihab Ad Din* Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhmmad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haythami Al Makki Al Ansari Al Shafii.

Maarufu kama Imam Ibn Hajar Al Haythami ambae alizaliwa Misri mnamo mwaka 1503 na alifariki mnamo mwaka 1566.Na alikua ni Mwanafunzi wa *Shayh ul Islami* Imam Zakarriyah Al Ansari na *Shaykh ul Islami*Imam Shihab Ad Din Al Ramli.

Na bila ya shaka tunapomzungumzia Imam Ibn Hajar Al Haythami basi pia Tunamzungumzia Imam mwenye Ilm ya kujua Fatwa za Maimam wote aaliotangulia kabla yake, yaani katika Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab mengineyo hakuna anaempata kwa ukubwa wa Ilm yake kuhusiana na Fatwa na Hadith.

Na hivyo mtu akitoa hoja basi nawe ukajibu kwa uthibitisho wa kusema kua kuhusiana na hili basi Imam Ibn Hajar Al Haytam amesema hivi basi hua umemaliza mada.Lakini haya yote kwa wanaojua tu, kwani wasiojua basi watakusumbua.

Naam, hivyo anasema Imam Ibn Hajar Al Haythami katika *Tuhfah Al Muhtaj Bi Sharh Al Minhaj* kuhusiana na *Bismi Allahi Rahmani Rahim* kabla ya Surat Al Fatiha kua:

عن أبي هريرة رضي الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: إذا قرأتم: الحمد لله فاقرءوا: ﴿بسم الله الرحمن الرحيم﴾ إنها أم القرآن، وأم الكتاب، والسبع المثاني، و﴿بسم الله الرحمن الرحيم﴾ إحداها

‘Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Amesema*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:Mnaposoma *Alhamd lillahi Rabbi Al Alamiin* (Surat Al Fatiha) basi anzeni na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim,* kwa Sababu *Bismi Allahi ni Ummu Ul Qur'an ni Ummu Ul Kitab na Sabaa Al Mathani* na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni moja kati ya Aya zake’*(*Imam Al Bayhaqi na Imam Daraqutni)*

Na tuliona kuhusiana namtizamo wa Imam Al Jazari na Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Musa Al Shatibi Al Andalus Al Malikikua wanakubaliana kua Unaweza kuisoma Surat At Tawbah kuanzia Aya ya pili na ukaanza na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* lakini si kwa aya yake ya Kwanza. Na hivyo basi tunarudi tena kuangalia mtizamo huu kwa Imam wa Wahakikishaji na Imam wa Ilm ya Fatwa za Wanazuoni yaani

Mujtahid Imam Ibn Hajar Al Haythami ambae yeye anatuambia kua: **‘Miongoni mwa Viongozi wa Wanazuoni wa Ilm ya Kisomo cha Quran, Imam Al Sakhawi amesema kua: ‘Hakuna kutofautiana juu ya Wanazuoni kuhusiana na kua ni Sunnah kuanza na Bismi Allahi Rahmani Rahiim unapoanza kusoma maanzoni mwa Surat At Tawbah, kwa ajili ya kutofautisha baina ya kuanzia mwanzoni mwa Sura na kuanzia kati kati ya Sura hio.’**

‘Lakini sasa hata hivyo Maelezo yake haya yamepingwa, Na miongoni mwa Wanazuoni wa Kisomo cha Qur'an aitwae Al Jabari, na hii ni kwa sababu jambo hili hua ni Makruh kwani Bismi Allahi haitakiwi kusomwa mwanzoni mwa Surat At Tawbah kwa sababu Aya hio imekuja na Upanga na kuwadhihirisha Wanafiq na Maovu yao tofauti na Sura nyenginezo, na mada hii

imezungumziwa kila sehemu katika Surat At Tawbah, Hivyo haitakiwi kusoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* hata kama mtu ataanza kusoma Aya ya katikati ya Sura hii kama vile ambavyo ilivyokua haikuamrishwa kusomwa mwanzoni mwake'*(Fatawa Al Fiqhiyyah)***

Na amesema Jarrah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kua**: *'Bismi Allahi RahmaniRahiim* ni Aya au ni Sehemu ya Aya katika kila Sura isipokua *Surat Baraah* na Mtizamo huu umenasibishwa kwa Wasomaji Qur'an wa Mji wa Makkah na Wanafiqh wa Mji wa Kufah. Ambapo Mtizamo huu pia umenukuliwa na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu* na Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu.*Na Mtizamo huu pia umenukuliwa na Imam Makhul, Imam Al Zuhri, Imam Ataa, Imam Tawus na Imam Said Ibn Jubayr.'**

Mtizamo huu pia Ndio mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii na Imam Abd Allah Ibn Mubarak. Na Hadith hii aliyoinukuu Imam Ibn Hajar Ibn Haythami na kuihakiki iliyopitia kwa Imam Ad Daraqutni, basi ni Hadith ambayo pia ni maarufu kwa Imam Abu Hanifa, Imam Sufyan Ath Thawry Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh na Imam Al Awzai.

Na mbali ya Hadith hii ambayo ndio inayotumika zaidi kama uthibitisho kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua *Bismi Allahi Rahmani Rahiim inatakiwa* isomwe ndani ya Sala kabla ya kusoma Surat Al Fatiha, lakini pia kuna hadith nyengine isemayo kua:

عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ، قَالَ كَانَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم لاَ يَعْرِفُ فَصْلَ السُّورَةِ حَتَّى تُنَزَّلَ عَلَيْهِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

'**Amesema Abd Allahu Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua hawezi kutofautisha baina ya Sura mbili tofauti hadi pale anaposhushiwa Maneno Bismi Allahi Rahmani Rahiim ndio hujua'***(Sunan Abu Daud)***

Ambapo Hadith hii imetumia maneno *Hatta Tunazila Aalayhi Bismi Allahi Rahmani Rahiim* yaani hadi anaposhushishiwa *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* maneno ambayo yanamaanisha kua *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ilikua ikishushwa katika kila wakati inapohushwa Sura mpya.Na hivyo *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ilikua ni aya inayowekwa mwanzoni mwa Sura kutokana na amrisho la *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na katika kuthibitisha hili pia basi kuna hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* Ambayo inasema: '**Siku Moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua pamoja nasi, na mara akalala, halafu akanyanyua kichwa chake huku akitabasam, hivyo nasi tukamuuliza: 'Ya Rasul Allah, hivi ni nini kinachokuchekesha?**

Ambapo nae akasema: Kuna Sura ambayo nimeshushiwa, inasema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim, Inna Aataynaka al Kawthar*! Hadi akimaliza Sura hio. ***(Sunan Abu Daud)***

Na katika Sahih Muslim kuna Hadithi isemayo kua:

سَمِعْتُ أَنَسَ بْنَ مَالِكٍ، يَقُولُ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم '' أُنْزِلَتْ عَلَىَّ آنِفًا سُورَةٌ '' . فَقَرَأَ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ حَتَّى خَتَمَهَا

Amesema Anasa Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu*kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*alisema kua: 'Kuna Sura ambayo nimeshushiwa, inasema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim, Inna Aataynaka al Kawthar*! Hadi akimaliza Sura hio*(Sahih Muslim)***

Na bila ya ya shaka ile Hadith ya Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* aliyouliziwa kuhusiana na kisomo cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo nae aliesema kua: **'Kilikua:**

(بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلا الضَّالِّينَ)

Bismi Allahi Rahmani Rahiim, Alhamd lillahi Rabbi Al Aalamiin, Ar Rahmani Rahiiim,Maliki yawmi Al Ddin hadi mwisho wa Surat Al Fatiha ambapo hii ni hadith iliyonukuliwa na Imam At Tirmidhii, Imam Ibn Huzaymah, Imam Ahmad, Imam Abu Daud, Imam Al Hakim na Imam Ad Daraqutni.

Hivyo anasema Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '***Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni Aya miongoni mwa aya za Surat Al Fatiha, na hivyo yeyote yule asieisoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* basi hujibatilishia Sala yake, na hii ni kutokana na kua ai mwenye kuikamilisha Surat Al Fatiha. Kwani ukiwacha neno Moja tu kutoka katika *Surat Al Fatiha* iwe kwa kusahau au kwa makusudi basi Rakaa ya Sala yako haihesabiwi***(Kitab Al Umm)**

Imam Muhammad Idris Al Shafii anaendelea kusema kua:**''Hivyo *Bismi Allahi Rahmani Rahim* ni lazima isomwe kwa Imam na Maamuma pia. Ambapo kwa upande mwengine basi kama Maamuma atamkuta Imam anarukuu, na kisha nae akaingia kwenye Ihram na kusema Allahu Akbar na kisha akarukuu na kisha kunyanyuka nae Imam basi katika hali kama hii ndio inapokua Maamuma Inamtosheleza Surat Al Fatiha ya Imam wake.'**

Ambapo huo ndio Mtizamo wa Vitabu vyote vya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii.Na akasema Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Kila Jambo Muhimu ambalo halianzi na *Bismi Allahi Rahmani Rahim* basi hua ni lenye kukatishwa (Kutokukubaliwa) na hii imenukuliwa na Imam Abu Daud na Imam Ibn Salah na wengineo wamesema kua ni *Hasan Hadith'***(Asna Matalib)**

Na kwa upande wa Imam Abd Allah Ibn Ab Rahman Ba Fadhl Al Hadhrami Al Shafii kua: '***Bismi Allahi Rahmani Rahim* ni Aya ya Surat Al Fatiha, na miongoni mwa masharti yake ni Aya zake zote za Surat Al Fatiha zintakiwa zisomwe, tena katika kisomo ambacho Msomaji atakua ni mwenye kujisikia mwenyewe kua anasoma kila herufi ya Surat Al Fatiha.Na inapendekezwa kusomwa kwa Sauti katika Rakaa mbili za Alfajir, na katika Rakaa mbili za Mwanzoni za Sala wa Magharibi na Isha.**

Na inapendekezwa kusomwa kimya kimya katika Sala nyenginezo, na kama mtu akisoma kimya kimya kwenye Sala ya Sauti au kwa sauti kwenye Sala ya Kimya bila ya kua na sababu yeyote inayokubalika kishariah basi jambo hilo hua linakirihisha.'***(Bushra Al Karim)***

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam Muhyi ad Din Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi anasema kua: **'Kutamka *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kwa sauti katika Sala ni Jambo linalopendekezwa na Wanazuoni wengi miongoni mwa Masahaba na waliofuatia baada yao. Miongoni mwaAbu Bakr As Siddiq, Umar Ibn Al Khattab, Uthman Ibn Affan, Ali Ibn Ab Talib, Amar Ibn Yasir, Ubay Ibn Kaab, Abd Allah Iban Abbas, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum, Al Qadhi Abu Tayyib* na**

wengineo, ambapo amesema Ibn Abi Layla kua: 'Hukumu yake jambo hili ni kusema kwa sauti au kwa kimya kimya, kwani vyote hua ni sawa.''

Mbali ya kua Imam Muhammad Idris Al Shafii ni mwenye Mtizamo wa kua *Bismi Allahi RahmaniRahiim* ni lazima isomwe kwa sauti katika Sala za Sauti.Lakini hata hivyo wakati Imam Al Shafii alipotembelea Mji wa Baghdad kwa wanafunzi wa Imam Abu Hanifa na kuwadia mda wa kusali Sala ya Maghrib na Imam Al Shafii akapewa asalishe basi hakusoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kwa Sauti.Na baada ya Sala alipoulizwa kwanini hakusoma kwa Sauti *Bismi Allahi Rahmani Rahim*na hivyo kua ni mwenye kuenda kinyume na mtizamo wake basi Imam Muhammad Idris Al Shafii alisema:**'Kwa Sababu hapa Pembeni kuna Kaburi la Imam Abu Hanifa, nae hakua ni mwenye kuisoma kwa Sauti, hivyo mimi nilisoma kimya kimya kwa kumheshimu Abu Hanifa, kwa sababu Maiti hua wanatusikia.'**

Amesema Imam Jafar Al Sadiq kua: **'*Bismi Allahi Rahmani Rahiim* ni aya kubwa sana katika kitabu cha Qur'an.'**

Na pia anasema Imam Ibrahim An Nias kua: **Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Amesema Malaika Jibril kua amesema Malaika Mikail kua amesema Malaika Israfil kua: Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

Ewe Israfil hakika mimi nnapa kwa Ukubwa wa uwezo wangu, na Mamlaka yangu na Ufalme wangu kua: Kama Mtu atasoma *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* pamoja na Surat Al Fatiha, basi kua shahidi wangu kua mimi hua ni mwenye kumsamehe mtu huyo madhambi yake na hua ni mwenye kumkubalia Mema yake

Hakika Mimi sitouunguza Moto Ulimi wa Mtu aliesema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim*, na nitamlinda kutokana na Adhabu ya Kaburi na Adhabu ya Moto katika Siku ya MalipoNitamuepusha Mtu huyo Na Khofu kubaa ya Siku hio,na hivyo atakutana nami kabla ya kukutana na Mitume na Mawalii wote.*(Kashif Al Libas)*

Naam..tumemalizana na Tasmiyah na tunaingia kwenye Nguzo ya nne ya Sala ambayo ni Kisomo cha Surat Al Fatiha katika Sala.

4 - QIRAAT SURAT AL FATIHA

❖❖❖❖

﴿وَلَقَدْ اٰتَيْنٰكَ سَبْعًا مِّنَ الْمَثَانِيْ وَالْقُرْاٰنَ الْعَظِيْمَ﴾

Walaqad <u>a</u>tayn<u>a</u>ka sabAAan mina almath<u>a</u>nee waalqur-<u>a</u>na alAAa<u>*Dh*</u>eema*(Surat Al Hijr 15:87)**

*Tafsir:**Na kwa hakika Tumekupa Mathani Saba na Qur'an Tukufu.***

Aya imetumia neno Mathani linatokana na neno Thana ambalo ni lenye kumaanisha kukunja, kurudia, kueguzia sehemu moja ya kitu juu ya chengine, kurudia rudia sehemu ya kitu, kukusanya pembe moja ya kitu na kuiweka juu ya nyengine au kuiunganisha na nyengine. Na hivyo Sabaa al Mathani hua linamaanisha Mambo Saba au Vitu Saba vinavyorudiwa rudiwa, ambapo tunapozungumzia kuhsiana na Qur'an basi tunaona kua vitu hivyo si vyengine vyovyote isipokua ni Aya au Sura Saba maalum za Qur'an.

Na ingawa kunamtizamo wa Kauli za upande wa baadhi ya Wanazuoni wa Tafsir kama Abd Allah Ibn Masud, Abd Allah Ibn Umar na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhum*ambao wamesema kua:**'Sabaa Al Mathani ni Sura zeye visomo virefu ambazo ni Surat AlBaqarah, Surat Al'Imran, Surat AlNisa',Surat AlMa'idah, Surat AlAn`am, Surat AlA`raf, na Surat Yunus ambazo ndani yake zimebeba Kanuni za Hukmu za Qur'an'** na miongoni mwa Maimam wanaounga mkno mtizamo huu ni pamja na Imam Sa`id Ibn Jubayr, Imam Mujahid na Imam Ad Dahhak.

Na pia kuna wasemao kua ***Sabaa Al Mathani ni SuratAl Baqarah, Surat Al Imran, Surat An- Nisa, Surat Al Ma'idah, Surat AlAn'am, Surat Al A'raf, na Surat Al Anfal pamoja na Surat At Tawba.***

Lakini pia kuna Mtizamo wa kauli nyengine zitokazo kwa Amir ul Muumini Umar Ibn Al Khattab, 'Ali Ibn Abi Talib, Ubay Ibn Ka`b, Abd Allah Ibn Mas`ud, Abd Allah Ibn Ibn 'Abbas*Radhi Allahu Anhum*, na Imam Hasan, na pia Imam Mujahid kua *Sabaa Mina Al Mathani* ni Surat Al Fatiha.

Na hivyo haishangaza kuona kua Imam Ibn Kathir amesea kua: **'Mitizamo yote miwili inaweza ikawa sahih kwa sabbu Sur azote zilizotajwa ni zenye kurudiwa rudia na ni zenye kua na sifa zinazofanana, yaani kama vile kwa mfano wa Misikiti miwili ambayo ni Msikiti wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wa Madina na Masjid Quba, ambapo alipokua akiulizwa baadhi ya wakati basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua Msikiti wangu ni Msikiti uliojengwa Kwa Taqwa, na pia alisema pia kua Masjid Quba ni Msikiti uliojengwa kwa Taqwa'**

Na hapo hapo mtizamo wa kua Sabaa Al Mathani ni Surat Al Fatiha ni Mtizamo unaotokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambayo alisema: **'Ummu ul Kitab ndio *Sabaa Al Mathani* na ndio Qur'an Tukufu***'(Sahih Buhari)*Na miongoni mwa sababu ya kua Surat Al Fatiha inaitwa Sabaa Al Mathani ni kua:

Kwanza Inasomwa katika kila Sala, ikimaanisha kuwa inasomwa katika kila rakaa.

Pili: Imam Al Zajjaj amesema kua: Imeitwa Al Mathani. Kwa sababu ni Sura inafuatiwa na inayosomwa pamoja nayo.

Tatu: Aya za Al Fatihah zinaitwa Mathani. Kwa sababu imegawanyika sehemu mbili, na dalili yake ni ile iliyopokewa kwamba Mtume, Sala na amani zimshukie, amesema: "Anasema Allah Subhanah wa Ta'ala Mtukufu: Nimeigawanya Sala baina yangu na mja wangu katika sehemu mbili. " katika hadith Al Quds ambayo tutaifafanua baadae

Nne: Iliitwa Mathani; Kwa sababu ina sehemu mbili: sifa na dua, na pia nusu yake ya kwanza ni haki ya Muumba ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* , na nusu ya pili ni haki ya Kiumbe, ambayo ni dua.

Tano: Al Fatihah inaitwa Al Mathani. Kwa sababu iliteremka mara mbili, mara moja katika mji wa Makka mwanzoni mwa Qur'an, na mara moja katika Mji wa Madina.

Sita: Inaitwa Al Mathani. Kwa sababu maneno yake ni yenye kujirudia na kiufafanuzi, kama vile: "Mwingi wa rehema, Mwingi wa kurehemu, Wewe tunakuabudu na Wewe tunakuomba msaada, utuongoze kwenye njia iliyonyooka, njia ya wale uliowaneemesha," na katika usomaji wa Omar. : "Sio wale ambao umewakasirikia na sio walio potea."

Hivyo amesema tena*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*inaelezea kuhusiana na umuhimu wa Surat Al Fatiha katika Ibada ya Sala kama ifuatavyo:

عَنْ عُبَادَةَ بْنِ الصَّامِتِ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ لَا صَلَاةَ لِمَنْ لَمْ يَقْرَأْ بِفَاتِحَةِ الْكِتَابِ وَسَلَّمَ

Amesema Ubaydah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu kua: Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua:* '**Hana Sala yeyote Yule asiesoma Fatihat Al Kitab (Surat Al Fatiha)**'*(Sahih Muslim)*

Na kutokana na Hadith hii basi ndio tunaona kua Surat Al Fatiha ni moja kati ya Nguzo za Sala.Na juu ya Usahih wa Hadith hii na juu ya Hili wanakubaliana Wanazuoni wa Madhhab yote ambayo katika Ibada yao ya Sala wanaelekea Kibla cha Al Kaabah katika Msikiti wa Makkah.

Kwani amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Katika Kila Rakaa ya Sala hua mna kisomo, hivyo kile ambacho *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitochutufanya sisi tukisikie basi na sisi tumekufanyeni nyinyi mkisikie.'**

Na kile alichokisoma kwa kimya kimya nasi tumesoma kimya kimya, hivyo yeyote yule atakaesoma Surat Al Fatiha, basi itamtosheleza na atakaesoma zaidi yake kwa kuongezea basi hua bora kwake*(Bukhari na Muslim)*

Ambapo amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: Maana ya maneno yasemayo:**'Yeyote yule atakaesoma Surat Al Fatiha basi itamtosheleza lakini atakaesoma zaidi hua ni bora kwake' yanamaanisha kua kusoma Surat Al Fatiha Katika Sala hua ni Wajibu,na hivyo Sala hua ni batili bila ya kisomo cha Surat Al Fatiha Na pia yanamaanisha kua Kusoma Sura nyengine baada ya Surat Al Fatiha hua kunapendekezwa, na kuna makubaliano juu ya hilo kuhusiana na Sala ya Al Fajr, Salat Al Jumaa na Rakaa mbili za mwanzo za Kila Sala,Na hua ni Sunna kusoma Sura nyingine baada yake kulingana na Mitizamo ya Madhhab yote. Ambapo Qadhi Iyyad amenukuu kutoka kwa Imam Malik kua ni Wajib kusoma Sura nyengine baada ya Surat Al Fatiha, na huu ni mtizamo sio***(Sharh Sahih Muslim)***

Ambapo amesemaAbu Huyayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

من صلى صلاة لم يقرأ فيها بأم القرآن فهي خداج » :عن أبي هريرة عن النبي صلى الله عليه وسلم قال اقرأ بها في نفسك، فإني سمعت :فقيل لأبي هريرة: إنا نكون وراء الإمام؟ فقال «–ثلاثًا– غير تمام قال الله تعالى: قسمت الصلاة بيني وبين عبدي نصفين، » :رسول الله صلى الله عليه وسلم يقول قال الله تعالى: حمدني عبدي، وإذا {الحمد لله رب العالمين} :ولعبدي ما سأل، فإذا قال العبد مجدني :، قال{مالك يوم الدين} :قال الله تعالى: أثنى علي عبدي، وإذا قال {الرحمن الرحيم} :قال قال: هذا بيني وبين {إياك نعبد وإياك نستعين} :فإذا قال –عبدي –وقال مرة فوَّض إلي عبدي اهدنا الصراط المستقيم صراط الذين أنعمت عليهم غير } :عبدي، ولعبدي ما سأل، فإذا قال قال: هذا لعبدي ولعبدي ما سأل {المغضوب عليهم ولا الضالين

‘***Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua: Yeyote atakaesali Sala bila ya kusoma Surat Al Fatiha*** **basi Sala yake ni BatilAmbapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliyarudia maneno haya mara tatu’**

Hivyo Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu akaulizwa: ‘***Jee vipi kama ikiwa tupo Nyuma ya Imam? Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*akajibu:Isome Mwenyewe ndani ya Nafsi yako**. **Kwani kwa hakika mimi nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua:*Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua:Hakika mimi nimeigawa Sala baina yangu na baina ya Mja wangu katika sehemu Nusu mbiliNa Mja wangu atakipata kile anachokiomba, anaposema:**

﴿ ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَالَمِينَ﴾

Alhamd lillahi Rabbi Al Alamiin **basi *Allah Subahanh wa Ta’ala* husema Mja wangu amenisifu.**

Na anaposema

﴿ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ﴾

Ar Rahmani Rahiim **basi *Allah Subahanh wa Ta’ala*husema Mja wangu amenitukuza**

Anaposema

﴿ مَٰلِكِ يَوۡمِ ٱلدِّينِ﴾

Malik yawmi Ad Din **basi *Allah Subahanh wa Ta’ala* husemaMja wangu amenitukuza**

Na anaposema

﴿ إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ﴾

Iyyaka Naabudu wa Iyyaka Nastain **basi *Allah Subahanh wa Ta’ala*husema Hili ni baina yangu na Mja wangu hivyo niombe nami nitakupa.**

Anaposema:

﴿ ٱهۡدِنَا ٱلصِّرَاطَ ٱلۡمُسۡتَقِيمَ۞ صِرَاطَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ ٱلۡمَغۡضُوبِ عَلَيۡهِم وَلاَ ٱلضَّآلِّينَ﴾

Ihdinaa Sirrata Al Mustaqiim, Sirat Alladhiina An Aamta Alayhim Ghayril Al Maghdhuubi wala Dhaliin**Basi *Allah Subahanh wa Ta’ala*Husema : Hili ni kwa ajili ya Mja wangu, na Mja wangu atakipata kile anachokiomba.’***(Sahih Muslim)*

Na tumeanza na Hadith hii kwa makusudi kwa sababu ndani yake Hadith ambayo ni yenye Kuzungumzia Surat Al Fatiha na pia ni yenye kuzungumzia Sala. Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema ndani yake kua: **‘Hakika Mimi nimeigawa Sala Katika Sehemu mbili.’**

Na kisha akaanza kuelezea kuhusiana na **Aya za Surat Al Fatiha** ambapo amesema kua Aya Tatu za Mwanzo ni kwa ajili yake na Aya ya nne kwa ajili yake *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kwa ajili ya Mja wake kwa sababu ni zenye kuonesha Unyenyekevu wa Mja katika kumtegemea Mola wake. Na kisha aya tatu za mwisho ni kwa Ajili ya Waja wake wanaoisoma Sura hio,au wanaoisali Sala husika.

Ambapo Idadi ya wingi wa Waja husika inaonesha kua namna watakavyokua Wamebarikiwa Waja hao kutokana na Kisomo chao. Kwa maana hio basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameinaasibisha Surat Al Fatiha na Sala. Na hivyo kuzungumzia Sala na kuifafanua Surat Al Fatiha ndani yake kwa sababu Surat Al Fatiha ndio Nguzo Kuu ya Sala. **Yaani Surat Al Fatiha ndio Sala yenyewe.**

Na ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: '**Hana Sala yeyote yule asiesoma Surat Al Fatih**a'*(Sahih Muslim).*

Hivyo Surat Al Fatiha ni Wajib kuisoma Katika Sala na hii pia ni kulingana na Madhhab yote.Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasimamia kama ilivyosema Hadith tuliyoanza nayo leo kua Maamuma pia anatakiwa asome Surat Al Fatiha yake **Na ndio Maana Maimam wanatakiwa watulie kidogo baada ya Kumaliza kusoma Surat Al Fatiha na Maamuma kuitikia Amiin**. **Na hii ni kwa sababu ya kuwapa mda Maamuma ili na wao kila mmoja apate kusoma Surat Al Fatiha yake.**

Ambapo amesema Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: **'Baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Malik wameyaelezea maneno haya ya Abu Hurayrah kuhusiana na Kusoma ndani ya Moyo, kua ni kama kuyafikiria maneno ya Surat Al Fatiha, kwa sababu unaposoma kitu ndani ya Moyo wako basi kitendo hicho hua hakiitwi kisomo kwa sababu ukweli ni kua mwenye kusoma hua ni mwenye kutumia Ulimi, hivyo kisomo hua ni kisomo pale ulimi unapokua unacheza cheza, na uthibitisho ya haya ni kua Wanazuoni wote wanakubaliana kua wakati Mwanamke anaokua katika siku zake basi hatakiwi kusoma kwa kutumia ulimi wake bali anaweza kusoma kwa kufikiria maana ya anachokisoma ndani ya Moyo wake.'**

Na amesema Ubaidah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Tulikua tunasali Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala ya Alfajir. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa anasoma Sura lakini ikawa vigumu kwake kusoma. Na baada ya kumaliza kusali, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** akauliza: **Inaonekana labda Mlikua mnasoma Nyuma ya Imam?'**

Ubayda Ibn Saamit *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: **'Sisi tukajibu Naam Ya Rasul Allah!'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema**: 'Msifanye hivyo isipokua kwa Surat Al Fatiha tu!Kwani Hakuna Sala kwa asieisoma Sura hio.'***(Sunnan Imam Abu Daud)*

Hadith inatuonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisalisha, na hivyo baada ya kumaliza kusoma Surat Al Fatiha na kisha kuanza kusoma Sura nyengine basi ikawa vigumu kwake kuupata Umakini wa Kisomo cha Sura husika kwa sababu ya Minong'ono ya Masahaba ambayo ilitokana na wao kua kila mmoja ni mwenye kusoma Sura yake baada ya kumaliza kusoma Surat Al Fatiha.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaambia kua Wasifanye hivyo isipokua kwa Surat Al Fatiha tu ambayo kila mmmoja anatakiwa aisome katika kila Rakaa iwe peke yake au na Imam iwe ni Sala ya Kimya au ni Sala ya Sauti.Na Hadithi hii imezungumzia Sala ya Al Fajir ambayo ni Sala ya Sauti.

Hii Hadith hii ni Sahih na Kulingana na vigezo vya Imam At Tirmidhii, Imam Al Bayhaqi, Imam Al Khattabi na wengineo.

Kwani anasema pia Imam Nuuman Ibn Thabit kua: '**Amesema Ataa Ibn Abi Rabah *Radhi Allahu Anhu* kua Masahaba Walikua wakisoma Surat Al Fatiha katika Kila Rakaa ya Sala.'**

Ambapo Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni Mwalimu wa Imam Abu Hanifa na alikutana na Masahaba zaidi ya 200 akiwemo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,*Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu,* Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu,* Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu,* Aisha *Radhi Allahu Anha*, Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* n.k

Na hakukutana nao tu, bali pia walikua ni Walimu wake waliompelekea yeye kua ni Mufti wa Mji wa Makkah katika kipindi cha Tabiina.Imam Ataa Ibn Abi Rabah *Radhi Allahu Anhu* alikua ni Mwalimu wa Imam Mujahid, Imam Ayub Al Sakhtiyani, Imam Amr Ibn Dinar, Imam Muhammad Ibn Is-haq, Imam Al Awzai, Imam Al Amash, Imam Abu Hanifa n.k

Ambapo anasema Imam Abu Hanifa kua: '**Sijawahi mimi kuona Mtu mwenye Ilm kama Ataa Ibn Abi Rabah.**' Imam Ataa Ibn Abi Rabih alikua pia mwalimu wa Imam Al Zuhri ambae ndie Mwalimu wa Imam Muhammad Idris Al Shafii.

Na nimemgusia Imam Ataa Ibn Abi Rabah ambae Mama yake alikua ni Muafrika kwa sababu tunapoiangalia Silsila ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa na pia ya Imam Muhammad Idris Al Shafii basi ndani ya Sanad za Hadith zao nyingi kuna Jina la Ataa Ibn Abi Rabah.

Na hivyo pia haishangazi kuona kua Mtizamo wa kua Surat Al Fatiha ni lazima kwa Anaesali aisome iwe kwa Sala ya Jamaa au ya Peke yake, iwe kwa sala ya Sauti au ya Kimya, ni Mtizamo waMadhhab ya Imam Abu Hanifa (kama ilivyotajwa katika *Mukhtasar Al Quduri*) na pia kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Kwani amesema Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu* kua:**'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Surat Al Fatiha na Sura nyengine katika Rakaa mbili za mwanzoni za Salat Adh Dhuhr, na Al Asr na Surat Al Fatiha peke yake katika Rakaa mbili za Mwishoni mwa Sala hizo.'***(Imam Ibn Rushd)*.** Ambapo huu ndio mtizamo wa Imam Malik.

Hivyo anasema Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua**: 'Ni Kawaida ya Wengi Miongoni mwa Waislam kua ni wenye kusoma baada ya Imam ndani ya Sala zao iwe katika Sala ya Sauti au ya Kimya Kimya**. **Ambapo Imam Al Bayhaqi amesema kua Huu ndio Mtizamo wenye Hikma na ndio Uliokua Sahih. Kisha Imam Al Bayhaqi akanukuu Hadith nyingi zenye Sanad kutoka kwa Umar Ibn Al Khattab, Ali Ibn Abi Talib, Abd Allah Ibn Masud, Ubay Ibn Kaab,Muadh Ibn Jabal, Abd Allah Ibn Umar, Abd Allah Ibn Abbas, Abu Dardaa, Anas Ibn Malik, Jabir Ibn Abd Allah, Abu Said Al Khudri, Ubaidah Ibn Samit, Abu Hurayrah, Hisham Ibn Amir, Imraan Ibn Husein, Abd Allah Ibn Mughafil na Aisha *Radhi Allahu Anhum*.Imam Al Bayhaqi kisha akasema kua: Nasi tumenukuu kutoka kwa Tabiina pia wakiwemo Urwa Ibn Az Zubayr, Makhuul, Ash Shabi, Said Ibn Jubayr na Hasan Al Basr***(Al Majmuu)***

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari kua:**'Kusoma Sura ndani ya Sala hua kunapendekezwa na hua kunapatikana kwa kusoma japo kusoma hata Aya moja ya Qur'an ndani yake. Hivyo katika Madhhab ya Imam Al Shafii basi Mtu anaesali Nyuma ya Imam katika Sala basi Surat Al Fatiha ni Wajib.Lakini baada ya Kusoma Surat Al Fatiha basi Maamuma anatakiwa akae kimya kama atakua anasikia Kisomo cha Imam. Na hii ni kwa *Sababu Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua:**

﴿وَإِذَا قُرِئَ ٱلْقُرْءَانُ فَٱسْتَمِعُوا۟ لَهُۥ وَأَنصِتُوا۟ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾

Waidha Quria Al Qur'anu FaistamiaAu lahu Waansituu LaAalakum Turhamnuna. *(Surat Al Aaraf 7:204)*

*Tafsir:**Hivyo Itakaposomwa Qur'an basi Isikilizeni na Kaeni Kimya ili mpate Kuingizwa kwenye Rehma.***

Imam Zakarriyah Al Ansari anaendelea kusema kua**: 'Inapendekezwa kusoma Surat Al Fatiha wakati Imam akiwa amekaa kimya na anapokua hasomi kwa sauti, kwani huu ndio mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni akiwemo Abd Allah Ibn Masud, Abd Allah Ibn Umar, Hisham Ibn Amir wote walikua wakisoma Nyuma ya Imam pale anapokua hasomi kwa sauti na Abd Allah Ibn Zubayr amesema kua: 'Imam akisoma kwa sauti basi wewe usisome, lakini kama ukiwa unakhofu kua hutowahi kusoma Surat Al Fatiha basi soma'**

Na kuhusiana nao mtizamo huu ndio kama alivyonukuu Said Ibn Musayyib, Said Ibn Jubayr, Al Hasan, Al Qasim Ibn Muhmmaad, Nafi Ibn Jubayr Al Hakam na Al Zuhri. Ambapo Abu Salamah Ibn Abd Rahman alisema kua: 'Imam hua ana mapumziko mawili, hivyo jinufaishe na Mapumziko hayo kwa kusoma Surat Al Fatiha pale anapoinga kwenye Sala. Na pale anaposema *Ghayri Al maghdhuubi Aalayhim wa Al Dhaliin'*

Na Urawah Ibn Zubayr alisema: 'Ama kuhusiana na mimi hua ni mwenye kujichukulia vitu viwili kutoka kwa Imam pale anaposema *Ghayri Al maghdhuubi Aalayhim wa Al Dhaliin'* basi hua nnasoma katika wakati huo na anapomalizia Sura hua nnasoma kabla ya yeye hajarukuu.''

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani kua: '**Wale wanaosema kua Maamuma hatakiwi kusoma kitu pale Qur'an inaposomwa ndani ya Sala, kama Wafuasi wa Imam Malik hua wananukuu Hadith isemayo kua**. **Anaposoma Imam basi sikilizeni kwa makini, hii ni Hadith Sahih katika Sahih Muslim kutoka kwa Abu Musa Al Ashari.'**

Ama kuhusiana na Hadith hii aliyoizungumzia *Mujaddid Ad Din* Imam Ibn Hajar Al Asqallani ya Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* basi hii ni ile Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا سَعِيدُ بْنُ مَنْصُورٍ، وَقُتَيْبَةُ بْنُ سَعِيدٍ، وَأَبُو كَامِلٍ الْجَحْدَرِيُّ وَمُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ الْمَلِكِ الأُمَوِيُّ - وَاللَّفْظُ لأَبِي كَامِلٍ - قَالُوا حَدَّثَنَا أَبُو عَوَانَةَ عَنْ قَتَادَةَ عَنْ يُونُسَ بْنِ جُبَيْرٍ عَنْ حِطَّانَ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ الرَّقَاشِيِّ قَالَ صَلَّيْتُ مَعَ أَبِي مُوسَى الأَشْعَرِيِّ صَلاَةً فَلَمَّا كَانَ عِنْدَ الْقَعْدَةِ قَالَ رَجُلٌ مِنَ الْقَوْمِ أُقِرَّتِ الصَّلاَةُ بِالْبِرِّ وَالزَّكَاةِ - قَالَ - فَلَمَّا قَضَى أَبُو مُوسَى الصَّلاَةَ وَسَلَّمَ انْصَرَفَ فَقَالَ أَيُّكُمُ الْقَائِلُ كَلِمَةَ كَذَا وَكَذَا قَالَ فَأَرَمَّ الْقَوْمُ ثُمَّ قَالَ أَيُّكُمُ الْقَائِلُ كَلِمَةَ كَذَا وَكَذَا فَأَرَمَّ الْقَوْمُ فَقَالَ لَعَلَّكَ يَا حِطَّانُ قُلْتَهَا قَالَ مَا قُلْتُهَا وَلَقَدْ رَهِبْتُ أَنْ تَبْكَعَنِي بِهَا . فَقَالَ رَجُلٌ مِنَ الْقَوْمِ أَنَا قُلْتُهَا وَلَمْ أُرِدْ بِهَا إِلاَّ الْخَيْرَ . فَقَالَ أَبُو مُوسَى أَمَا تَعْلَمُونَ كَيْفَ تَقُولُونَ فِي صَلاَتِكُمْ إِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم خَطَبَنَا فَبَيَّنَ لَنَا سُنَّتَنَا وَعَلَّمَنَا صَلاَتَنَا فَقَالَ " إِذَا صَلَّيْتُمْ فَأَقِيمُوا صُفُوفَكُمْ ثُمَّ لْيَؤُمَّكُمْ أَحَدُكُمْ فَإِذَا كَبَّرَ فَكَبِّرُوا وَإِذَا قَالَ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلاَ الضَّالِّينَ فَقُولُوا آمِينَ . يُجِبْكُمُ اللَّهُ فَإِذَا كَبَّرَ وَرَكَعَ فَكَبِّرُوا وَارْكَعُوا فَإِنَّ الإِمَامَ

يَرْكَعُ قَبْلَكُمْ وَيَرْفَعُ قَبْلَكُمْ " . فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " فَتِلْكَ بِتِلْكَ وَإِذَا قَالَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ . فَقُولُوا اللَّهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ . يَسْمَعُ اللَّهُ لَكُمْ فَإِنَّ اللَّهَ تَبَارَكَ وَتَعَالَى قَالَ عَلَى لِسَانِ نَبِيِّهِ صلى الله عليه وسلم سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ . وَإِذَا كَبَّرَ وَسَجَدَ فَكَبِّرُوا وَاسْجُدُوا فَإِنَّ الإِمَامَ يَسْجُدُ قَبْلَكُمْ وَيَرْفَعُ قَبْلَكُمْ " . فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " فَتِلْكَ بِتِلْكَ . وَإِذَا كَانَ عِنْدَ الْقَعْدَةِ فَلْيَكُنْ مِنْ أَوَّلِ قَوْلِ أَحَدِكُمُ التَّحِيَّاتُ الطَّيِّبَاتُ الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ " .

Amesema Hatan Ibn Abd Allah Al Raqashi kua: 'Mimi nilikua nikisali pamoja na Abu Musa Al Ashari na wakati alipokua katika Qadah (Kika cha Attahiyat) basi mmoja kati ya watu akasema: 'Uqqirat Al salatu bi Al Birri wa Zakkatuh – Sala imefardhi shwa pamoja na Ucha Mungu na Zakkat'.

Hatan anasema kua: 'Baada ya Abu Musa kumaliza kusali a kutoa Salam basi akawageukia watu na kuuliza: 'Jee ni nani miongoni mwenu aliesema kadha wa kadha?' na ukimya ukatanda miongoni mwa watu, Abu Musa Al Ashari akauliza tena: 'Ni Nani miongoni mwenu aliesema kadhaa w kadhaa?' ukimya ukatanda miongoni mwa watu.'

Abu Musa akasema: 'Inawezekana labda ikawa ni wewe Hatanndie uliesema?' Hatan akajibu: 'La mimi sikusema kitu chochote, na nilikua nnakhofu kua huenda ukawa utakerekea kuhusiana na jambo hilo' hivyo mmoja miongoni mwa Watu akasema: 'Ilikua ni mimi hapa ndie niliesema, lakni sikukusudia ubaya wowote'

Abu Musa Al Ashari akasema: 'Hivi Jee hamjui nyinyi kile mnachotakiwa kukitamka ndani ya Sala? Kwani kwa hakika*Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*alitufahamisha sisi na kutuelezea namna ya Kusali kwa kusema: 'Mnaposal basi nyoosheni Safu zenu na mchaguei mmoja wenu awe Imam wenu. Kisha semeni Takbir pale anaposema Takbir, na anaposema *Ghayri Al Maghdhoubi Alahyhim wala Al Dhaliina,* basi semeni Amiin. Kwani Allah atakujibuni. Na Imam anaposema Takbir basi na nyinyi pia semeni Takbirkwani Imam hua anarukuu kabla yenu na anainuka kabla yenu.'

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kimoja hua ni sawia na chengine, na anaposema: '*Samia Allahu liman Hamida* basi nyinyi mnatakiwa mseme: '*Allahuma Rabbana wa laka al* Hamd' kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametuambia kupitia katika Ulimi wa Nabii wake *Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Allah Humsikiliza Yule anaemtukuza'na Imam anaposema Takbir na Kusjudu basi na nyie pia inabidi mseme Takbir na Kusjudu.' Kwani Imam hua ni mwenye kusjudu na kuinuka kabla yenu.''

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kimoja hua ni sawia na chengine, na Imam anapokaa Qa'da basi maneno ya mwanzo kwa kila mmoja miongoni mwenu yanatakiwa yawe: *Attahiiyat Al Tayyibat Al Salawwatu lilahi Salamu aAlayka Ayyuha Al Nabbiyu wa Rahmat Allahi Wabarakatuhu Asalamu aAlayka wa Aala Aaibadi llahi alssalihina Ash hadu an la Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhamamdan Abduhu wa Rasuluhu* – Matendo yote yaliyotekelezwa kwa Maneno, Vitendo vya Ibadan a kila kitu kizuri ni kutokana na Allah Usalama uwe juu yako Ewe

Nabii na Rehma na Huruma za Allah ziwe juu yako. Salama iwe juu yetu na juu ya waja wema wa Allah. Nashuhudia kua hakuna Mungu isipokua Allah Subhanah wa Ta'ala na nashuhudia kua Muhammad ni Mja wake na ni Mtume wake.'*(Sahih Muslim)*

Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani anaendelea kusema kua **'Na wale wanaosema kua Ni Wajib kusoma basi husema kua Ni Wajibu kusoma baada ya Imam kumaliza Kusoma Surat Al Fatiha na kabla ya kuanza kusoma Sura nyengine, hivyo inatakiwa kusomwa pale Imam anapokua amepumzika na kukaa kimya baada ya kusoma Surat Al Fatiha.Hivyo Maamuma hutakiwa Kusikiliza kwa umakini pale Imam anapokua anasoma, na Kisha Maamuma anatakiwa Asome pale Imam anapokua amekaa Kimya'***(Fath Al Barr)***

Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani anaendelea kusema katika Fath Al Barr kua:**'Na imethibitishwa kuruhusika bila ya kipingamizi kwa yule anaesali nyuma ya Imam kusoma Surat Al Fatiha katika Sala ambazo Qur'an hua inasomwa kwa sauti, katika Hadith iliyonukuliwa katika Sahih Bukhari katika mlango wa Juz Al Qiraa'ah na pia katika Al Tirmidhii, Ibn Hibban n.k kua kutoka Makhul, kupitia kwa Mahmud Ibn Al Rabii, kupitia kwa Ubaidah *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipata kigugumizi katika kisomo chake cha Salat al Fajr na hivyo alipomaliza kusoma basi akauliza: 'Inaonekana mlikua mnasoma nyuma ya Imam wenu'Masahaba wakasema: 'Naam' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Msifanye hivyo isipokua kwa kusoma Fatihat Al Kitab, kwani hakuna Sala kwa asieisoma.''**

Kwa maana hio basi hata kama Maamuma itakua hamsikii Imam basi Maamuma anatakiwa asome Sura baada ya Surat Al Fatiha.Ambapo hali hii ya kutomsikia Imam hua inategemea na Aina ya Sala yenyewe na pia hua inategemeana na hali ya mazingira husika katika wakati wa Sala husika.

Yaani kwa mfano Maamuma anasali Sala ya kimya kimya, labda Salat Dhuhr au Al Asr basi anatakiwa asome Sura nyengine kimya kimya baada ya Surat Al Fatiha. Kwani kwa upande mwengine basi amesema pia Imran Ibn Husein *Radhi Allahu Anhu* kua: **'*Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alikua akisalisha Salat Al Dhuhr, na kuna mtu nyuma yake akawa anasoma *Sabihisma Rabbika Al Aala.* Hivyo baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumaliza kusali basi akauliza: 'Jee ni nani miongoni mwenu aliekua akisoma *Sabihisma Rabbika Al Aala.*' Ambapo kuna Mtu akasema: 'Ni Mimi hapa ya Rasul Allah' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hakika mimi nilikua nadhani kua kuna mtu nabishana nae miongoni mwenu (wakati nilipokua nikisoma kisomo changu)**' *'(Sahih Muslim)*

Na pia kwa mfano anasali Sala ya Maghrib, au Isha au Al Fajr, au Ijumaa n.k ambazo ni Sala za Sauti. Lakini sasa katika Wakati Anasali Basi Maamuma akawa hakuweza kumsikia Imam, labda kwa sababu Umeme umekatika ghafla, na Spika hazifanyi kazi, au labda Maamuma yuko mbali na Hasikii Kisomo cha Imam labda kwa sababu Msikiti husika hauna Vipaza Sauti n.kBasi katika hali kama hii Maamuma anatakiwa asome Sura au Aya baada ya Surat Al Fatiha.

Ingawa kwa Mtizamo wa Imam Al Zuhr basi katika hali kama hii Maamuma pia hua anatakiwa asisome kitu chochote ambao pia ni mtizamo wa Imam Abu Hanifa, Imam Ahmad, Imam Malik na pia ndio uliokua mtizamo wa zamani (*Al Qawl Al Qadim)* wa Imam Muhamamd Idris Al Shafii kabla ya kubadilisha mtizamo katika katika *Al Qawl Al Mutammad.*

Ambayo ni yenye kusema kua: **'Ni wajib kwa wale wanaosali peke yao au katika Jamaa kua ni wenye kusoma Umm Ul Qura'an katika kila Rakaa, kwani vyenginevyo basi hua haitoshelezi kwa sababu hii ni nguzo ya Sala.'***(Kitab Al Umm)*

Kwani amesema Shaykh Ul Islam Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Yahya Sharaf An Nawawi kua:**'Surat Al Fatiha ni Wajib katika Kila Rakaa isipokua katika Rakaa ya Masbuq'***(Minhaj Talibin)*

Na hapa ametajwa Masbuq kwa sababu katika kila hatua ya Sala ya Jamaa hua kuna Maamuma wa aina mbili, ambapo aina ya kwanza hua anajulikana kama Muwafiq na aina ya pili hua ni Masbuq.Hivyo hata katika Kisimamo hua kuna:

1- Muwafik yaani Maamuma alieafikiana kiwakati na Imam na hivyo kua ni Mtu ambae amemuwahi Imam katika Kisimamo cha Sala husika na hivyo Maamuma huyo kua na mda wa kutosha wa kusoma Surat Al Fatiha ndani ya Kisimamo cha Sala husika.

2 - Masbuq yaani Maamuma aliechelewa yaani hakuafikiana kiwakati na Kisimamo cha Imam na hivyo katika kuchelewa kwake basi akawa ni mwenye kukosa mda wa kusoma Surat Al Fatiha ndani ya Rakaa ya Sala husika.

Na amesema *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* kua:**'Yeyote yule atakaemuwahi Imam akiwa katika hali ya Kurukuu basi hua ni mwenye kuiwahi Rakaa.'***(Imam Abu Daud)*

Na akasema Imam Ad Daraqutni kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua**: **'Yeyote Yule atakaejiunga na Sala wakati Imam yuko kwenye Rukuu, basi Rukuu hio haitohitaji kurudiwa nae.''**

Hivyo kulingana na hadith hii na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Maamuma huyu aliekua na Sifa ya Masbuq ya kutowahi kisimamo na kumuwahi Imam katika Kurukuu basi kwake yeye hua haihitajiki kusoma Surat Al Fatiha ya Rakaa hio bali kufunga Sala na kisha moja kwa moja kuingia kwenye Rukuu.

Na tunaporudia kwa Maamuma ambae ni mwenye sifa ya Muwafik basi hali yake hua ni kulingana na Kisomo cha Imam.Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi kila Imam katika Kusalisha kwake anatakiwa apumzike mara sita katika Kisimamo cha kila Rakaa kwa ajili ya Kumpa Maamuma nae wakati wa Kufanya Kisomo husika katika Kisimamo.

Kama anavyosema Imam Ibrahim Ibn Muhammad Ibm Ahmad Al Safi A Bajuri Al Misri Al Shafii kua: **'Ni Sunnah Mandub (Sunnah Inayopendekezwa) Kua na Pumziko dogo baina ya hatua zifuatazo:**

1-Baina ya Taharrum na Tawajh - yaani Baina ya Takbir ya Kuingia kwenye Sala na Dua ya Ufunguzi wa Sala.

2-Baina ya Tawajjuh na Taawudh - yaani Baina ya Dua ya Ufunguzi wa Sala na Audhu Bi Allahi Minna Al Shaytani Rajiim.

3 - Baina ya Taawudh na Bismi Allah - Yaani baina ya Audhubi Allahi mina Al Shaytani Rajiim na Bismi Allahi Rahmani Rahiim.

4-Baina ya Surat Al Fatiha na Amiin - yaani baina ya Kusoma Surat Al Fatiha na Kuitikia Amiin.

5-Baina ya Aamiin na Sura yaani baina ya Kuitikia Amiin ya Surat Al Fatiha na kusoma Sura nyengine.

6-Baina ya Sura na Takbirat Al Rukuu - Yaani Baina ya Kumaliza kusoma Sura iliyofuatia baada ya Surat Al Fatiha na Kurukuu.

Ambapo Imam Al Bajuri anaendelea kutuambia kua: '**Hivyo Kuna mapumziko sita ambayo yanapendekezwa katika Kusimamo cha Rakaa ya Sala**. **Ambayo Imam anatakiwa asimame katika kila Pumziko kwa mda wa kiasi cha kusema Subhana Allah**, **Isipokua katika Pumziko la baina ya Amiin na Sura inayofuatia baada ya Surat Al Fatiha ambapo Imam anatakiwa apumzike ili kumuachia Maamuma asome Surat Al Fatiha yake.Ambapo katika Pumziko hilo basi Imam pia nae anapendekezewa awe anasoma Sura au Dua kwa siri ndani ya Moyo wake, lakini kama akisoma Qur'an basi hua ni bora zaidi.'**

Imam Al Bajuri anaendelea kusema kua: '**Hivyo maana ya pumziko hapa hua halimaanishi kua Imam asome kwa Sauti hicho anachokisoma kwani akifanya hivyo basi itakua si pumziko ambalo ni lenye kutakikana katika Kisimamo cha Sala**. **Ambapo Pumziko hilo hua ni sawa na Pumziko lile la Imam anaesalisha katika Sala ya Khofu anapokua anakisubiri kikundi cha Maamuma wa pili kuanza kwenye Rakaa ya pili ya Salat Al Khawf.'***(Hashiyyah Al Bajuri)*

Hivyo pumziko la Kisomo cha Imam kwa ajili ya Maamuma kusoma Surat Al Fatiha hua lina umuhimu wake kiasi ya kua: **Hua halitakiwi kuachwa isipokua labda pale inapokua Imam anajua kua Maamuma wake hatoweza kumsikia katika kisomo chake kwa sababu ya kutokana na kua Maamuma huyo ni kiziwi***(Sharh Umdat Al Ahkami, Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Al Imad Al Aqfahsi Al Shafii)*

Na hivyo inapokua labda tuseme Maamuma anasali numa ya Imam anaesoma kwa kasi kwa mfano katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ambao ndani yake hua malipo makubwa sana ya kuanzia mara 70 kwa kila Ibada.Ambapo mbali ya kua Ibada maarufu ndani ya Mwezi huu hua ni Funga lakini pia hua kuna Ibada maarufu ya Salat Al Tarweh. Ambapo bila ya Shaka Miskiti Mingi yenye yenye Kusalisha Salat Al Tarweh ndani ya Mwezi wa Ramadhani hua ni ile Miskiti yenye kufuata Mfumo wa Madhhab ya Imam Al Shafii ya kusoma Surat Mufassalat au Sura ndogo ndogo kwa kuanzia katika *Surat Al Bayyina yaani Lam Yakuni Alladhiina Kaffaru.*

Ambao huu ni Mfumo wa Asili unaofuatwa na wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuanzia Misri,Makkah, Hadhramout, Afrika ya Mashriki hadi Mashariki ya Mbali kabla ya kuanza kwa huu mfumo wa Kisomo cha Juzuu nzima kwa Kila Siku.

Ambapo mfano huu wa aina hii ya Kisomo cha Sala ambacho mara nyingi Imam hua anatumia kasi ya Haraka katika Usomaji, na hivyo kumfanya Maamuma asiwe si mwenye kuweza Kusoma Surat Al Fatiha baada ya Surat Al Fatiha ya Imam. Basi tunapozungumzia katika Sala kama hii au Sala ya Imam ambae labda si Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii na hivyo baada ya Surat Al Fatiha hua hasimami kumpa Nafasi Maamuma kusoma Surat Al Fatiha.Basi Maamuma ambae ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii anatakiwa achukue moja kati ya hatua mbili zifuatazo ili aweze kua ni mwenye kuipata Nguzo ya Kisomo cha Surat Al Fatiha nyuma ya Imam kama huyu ambazo ni.

1-Maamuma anaruhusika Kusoma Surat Al Fatiha yake kimoyo moyo na kutumia Ulimi bila kutoa Sauti mara tu baada ya Imam kuanza Kusoma Surat Al Fatiha, lakini asiwe ni mwenye kuanza kumtangulia Imam katika Kisomo hicho.

2-Maamuma anaruhusika Kusoma Surat Al Fatiha yake Kimya kimya kwa Moyo na Ulimi baada ya Kuitikia Amiin ya Pamoja na kisha Imam akaanza kusoma Sura nyengine.

Na hii hali ya kisomo cha pili cha Maamuma hua inapendekezwa zaidi kuliko hali ya kwanza.Ambapo hii hali ya kisomo ya pili hua inajulikana pia kama Ta'akhir Al Fatiha yaani kuichelewesha Surat Al Fatiha kaa kuisoma sambamba na Kisomo cha Sura ya pili ya Imam.*(Fat-h Al Wahhab, Fat-h Al Muin)*

Na ingawa kuna baadhi wanaweza kua na wasi wasi juu ya hili na kutaka kuhoji kuhusiana na hukmu ya ile aya isemayo:

﴿وَإِذَا قُرِئَ ٱلْقُرْءَانُ فَٱسْتَمِعُوا۟ لَهُۥ وَأَنصِتُوا۟ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾

Waidha Quria Al Qur'anu FaistamiaAu lahu Waansituu LaAalakum Turhamnuna.*(Surat Al Aaraf 7:204)*

Tafsir: **Hivyo Itakaposomwa Qur'an basi Isikilizeni na Kaeni Kimya ili mpate Kuingizwa kwenye Rehma.**

Hivyo nawaomba wawe na Subra kwa sababu baadae tutakuja kuifafanua kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii juu yake.

Ambapo anasema Imam Al Shafii Al Saghir Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Ramli kua:**'Kama Maamuma atakua ni Muwafiq basi inapendekezwa kusoma Surat Al Fatiha pamoja na Imam pale atakapokua anajua kua hatofanikiwa kusoma Surat Al Fatiha baada ya kisomo cha Imam, na kama atakua ni Masbuq basi itakua ni Wajibu kwake kusoma Surat Al Fatiha pamoja na Imam'***(Nihyayat Al Muhtaj bi Sharh Al Minhaj)*

Kwani Anasema Shaykh Ul Islami Imam Al Shafii Al Saghir Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Ramli Al Shafii kua: '**Kama Maamuma atakua ni Muwafiq (alieafikiana na Imam kwa kuanza nae katika Kisimamo cha Sala) basi inapendekezwa kwake kusoma Surat Al Fatiha pamoja na Imam pale itakapokua Maamuma huyo anajua kua hatofanikiwa kusoma Surat Al Fatiha baada ya Kisomo cha Imam**. **Na kama Maamuma atakua ni Masbuq(Yaani aliechelewa kuwahi Kisomo cha Surat Al Fatiha cha Imam na hivyo kumkuta Imam ameshaanza kusoma Sura nyengine) basi hua ni Wajib kwa Maamuma kusoma Surat Al Fatiha pamoja na Kisomo cha Imam.***(Nihayat Al Muhtaj)*

Ambapo anasema Imam Al Bujaraymi **katika kuainisha kwake aina tano za Muqarana au Musawaqa yaani kitendo kinachofanywa wakati mmoja na Imam, basi ndani yake hua pia hiki kitendo cha Maamuma kusoma pamoja na Imam ambacho katika hali hii hua ni Wajib pale inapokua Maamuma anajua kua anatakiwa kufanya hivyo katika hali aliyokua nayo.***(Hashiya Al Bujaraimi)*

Na hii inaonesha kwa namna gani Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Walivyoamua kusimamia Mtizamo wa kuonesha Umuhimu wa Kusoma Surat Al Fatiha katika Kila rakaa ya Sala.

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Al Muhaqqiqin Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: **Kwa kua inajulikana kua Sababu ya Maamua kua ni mwenye kupendekezeshwa Kuichelewesha Surat Al Fatiha katika Mahali pake ni kutokana na tegemeo la Maamuma kua Imam atasita na kupumzika kidogo baada ya kusoma Surat Al Fatiha kwa ajili ya kumwachia Mda Maamuma Nae asome Surat Al Fatiha, Au labda Maamuma hua anategemea kua Imam**

atasoma Sura ndefu itakayompa nafasi na yeye kusoma Surat Al Fatiha yake. **Na Sababu ya Pendekezo la kua Imam anatakiwa asite na kupumzika ni kua Imam hua hawezi kujua kama Maamuma amesoma Surat Al Fatiha pamoja nae ama hakusoma na hivyo inabidi amsubiri ili asome.'***(Tuhfa Al Muhtaj)*

Kwani hapa tunaona namna Wanazuoni waliweka kanuni ya Ushirikiano na ufahamiano baina ya Imam na Maamuma katika Sala ya Jamaa.Na hii ndio maana ya Jamaa kwamba Kiongozi (Imam) ampe Nafasi Anaemfuata Nyuma yake (Maamuma) ili nae aweze kutekeleza wajibu wake kiibada.Na pia Anaefuata Kumpa Nafasi yake kiongozi wake kwa kumsubiri Imam wake amalize kisomo kisha na yeye ndio asome, isipokua pale inapokuandani ya Kisimamo kwa sababu tulizozitaja hapo kabla zitakazo mpelekea Maamuma kujitegemea kivyake katika Kisomo cha Surat Al Fatiha.

Ambapo hapa sasa mbali ya kua Maamuma alikua Muwafiq yaani aliewahi lakini itabidi awe Masbuq yaani aliechelewa katika kisomo kutokana na Kasi ya Kisomo cha Imam au kutopumzika kwa Imam baada ya Kusoma Surat Al Fatiha.,n.k

Ama kwa upande mwengine basi Maamuma anaweza kusoma Surat Al Fatiha pamoja na Fatiha ya Imam (yaani, Musawaqa au Muqarana) au hata kumtangulia kabla Imam hajamaliza Fatiha yake ambapo hua kunajulikana pia kua kama ni Musabaqa hua inaruhusiwa kwa sababu kumtangulia Imam katika Rukn Qawli yaani Nguzo ya Kauli hua shakuna madhara katika Sala kuliko kumtangulia katika Rukn Fi'li yaani Nguzo ya Kitendo. Ambapo hata hivyo, hii haimaanishi kwamba haipendekezwi kabisa, kwani kila mara linapotumika neno 'hakuna madhara' katika Madhhab ya Imam Al Shafii basi kwa kitaalamu hali ya Hakuna Madhara basi hua inamaanisha kua ni Khilaf Awla yaani ni Tofauti inayothaminika au ni Tofauti bora ambayo humaanisha kua hua ni bora kutofanya hivyo lakini hapo hapo kufanywa kwake jambo husika hua hakubatilishi Ibada husika.

Ambapo hua ni jambo la kawaida katika Madhhab ya Imam Al Shafii kama vile ilivyokua kwa Madhhab mengine yote kua kwa baadhi ya Mtizamo hua ni yenye kupingana na ndio maana ikawa kuna Qawl Mutamamd yaani Kauli inayotegemewa na kukubalika zaidi na Wengie miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na pia hua kuna Al Qawl Al Mashhur yaani inayojulikana lakini haikubaliki na Wanazuon wengi kutokana na kua ni yenye kukubalika na Imam Mmoja au Maimam kidogo sana kiidadi ndani ya Madhhab.

Ambapo kuhusiana na jambo hili la Maamuma kusoma pamoja na Imam basi tunaona kua kuna Qawl Mashhur ambayo si Qawl Mutamamd ambayo inasema kua inapokua Maamuma kwa njia moja au nyengine amekua ni mwenye kumtangulia Imam katika kisomo cha Surat Al Fatiha basi hua ni Wajibu kwake Maamuma kuirudia Surat Al Fatiha wakati Imam anaendelea kusoma Surat Al Fatiha au baada ya Imam kumaliza kisomo hicho ambako hua ni bora zaidi.

Wakati *Qawl Al Mutammad* hua ni *Mandub* kwa Maamuma kuirudia Surat Al Fatiha yake, Na hivyo kutokana na hali hii basi Wanazuoni wa Mwishoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanaichukulia hukmu ya asili katika jambo hili kua ni ya Khifal al Awla yaani ile ya Tofauti iliyokua bora kama alivyosema *Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Al Imad Al Aqfahsi Al Shafii* katika *Qawl Tamm,* ili kutofautisha tofauti hizi basi ndio ikawa katika Madhhab ya Imam Al Shafii kuna Hukmu ya kuchelewesha kisomo cha Surat Fatiha ya Maamum mpaka baada ya Imam (yaani, Ta'khir Al Fatiha) kua ni kitendo kilichopendekezwa zaidi pale inapokua Maamuma anatarajia kusoma Surat Al Fatiha katika wakati wa pumziko la Imam kwa ajili yake au katika wakati wa kisomo cha Imam cha Sura .

Na hivyo kwa ufupi, kama ikiwa kuna sababu fulani nzuri inayokubalika, ambayo itampelekea Maamumakuona kua hafikirii kwamba ataweza kusoma Fatiha katika wakati wa kisomo cha Imam cha Sura cha baada ya Surat Al Fatiha, basi kwa Maamuma kusoma Surat Fatiha pamoja na Imam hua ni hali yenye kisingizio kinachokubalika kwa upande wa hukm ya asili ya Khilaf Awla kama tulivyoona katika kuelezea kwetu hapo kabla. Na kama Ikitokea hivyo, na Maamuma akaamua kusoma Surat AlFatiha huku Imam akiwa anasoma Surat AlFatiha, basi hua ni bora kwa Maamuma kua aanze kusoma Surat Al Fatiha yake mara tu baada tu ya Imam kuanza kisomo chake cha Surat Al Fatiha yake ili asije akamtangulia Imam katika usomaji wake huo wa Surat Al Fatiha, kama ilivyo katika Rukn Fi'li Nguzo ya Kivitendo, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie pekee ndiye anayejua zaidi!

Ama kwa upande mmmoja tunapofuatilia zaidi kwa kumuangalia Al Muhaqqiq Imam Ibn hajar Al Hatyami basi hua tunaona kua kulingana na hali na mazingira tofauti basihua inawezekana kwa hadhi ya Maamuma kua ni yenye kubadilika baina ya kuwa ni hali ya Muwafiq na kungia katika hali ya Masbuq katika wakati wowote ndani ya mojawapo ya rakaa nne za Sala, kwani ni kawaida kwa mtu anapokua anasali pamoja na Imam kwa kumuwahi tangu mwanzoni sambamba kuanzia kwenye Takbrat Al Ihram, na hivyo Maamuma kua ni Muwafiq pale inapokua Kisomo cha Imam ni cha kawaida lakini kwa baadhi hutokea kua ni Masbuq kutokana na Kisomo cha Imam kua ni chenye kasi kusomwa kwa kasi zaidi na hivyo Kisomo husika hua kifupi kunakopeleeka Maamuma kushindwa kumalizia Kisomo cha Surat Al Fatiha.

Na kwa upande mwingine, hua ni kawaida pia kua kama ikiwa Ma'mum amechelewa kujiunga na Sala na hivyo kumkuta Imam akiwa katika nusu ya kisomocha Surat AlKafirun kwa mfano katika rakaa ya kwanza, na ambapo katika hali hii basi Maamuma atakuwa ni Masbuq. Ambapo hali hii hua ni tofauti kwa mfano mwengine wa Maamuma aliejiunga na Sala katika wakati Imam akiwa anaanza kusoma kubwa zaidi kwa mfano Surat Adh Dhuha, ambapo katika hali kama hii basi Maamuma husika hua na Darja ya Muwafiq.

Hivyo haya yote hua yanategemeana na hali ya mazingira ya kua kama Maamuma atawahi kufanikiwa kukipata kisomo cha Imam husika, na hivyo kama ikiwa Maamuma atakua na shaka ya kama kwamba atakua ni Muwafiq au ni Masbuk basi kwake yeye Maamuma ni bora kuchukua tahadhari ya kujihesabu kua yeye ni Muwafiq na hivyo amalizie kisomo chake cha Surat Al Fatiha. Na hii ni kwa sababu ya kua kama ikiwa Maamuma atajihesabu kua ni Muwafiq basi basi atakua na udhuru ambao anaruhusika kua nao Maamuma mwenye uwezo wa kusoma Qur'an kidodogo kidogoSurat yake Al Fatiha yaani asiekua na kasi katika kisomo chake, na hivyo anaruhusika kuamalizia Kisomo chake.

Kwani kama akijihesabu kua ni Masbuq basi Maamuma hua ni mwenye kukosa ruhusa hio ya kuchelewa na hivyo humbidi kua ni mwenye kumfuata Imam katika kila herufi aisomayo, ambayo hio hua ni Qudwa Haqqiqiya.

Ambapo hali ya Qudwa Haqqiqiyah hua ni hali ya kusali nyuma ya Imam ambae anasoma kwa kasi kubwa sana katika kisomo chake, kiasi ya kua Maamuma anapokua amesimama kutoka kwenye Tashshahud ya kwanza au Sijda yake basi anamkuta Imam anakaribia kurukuu au tayari anarukuu na hivyo kua ni mwenye kukikosa kisomo cha Imam katika kisimamo chake, (hapa hua inambidi Maamuma kuachana na At Tahiyyat yake hata kama hajaimaliza, ili asihisabiwe kua ni mwenye kutofautiana an kumdharau Imam) na hivyo Maamuma anapokuja juu na kumkuta Imam anataka kurukuu basi Maamuma humbidi kutotakiwa kusoma Surat Al Fatiha bali anatakiwa moja kwa moja kurukuu pamoja na Imam na hivyo jukumu la Kisomo cha Surat Al fatiha ya Maamuma litakua limebebwa na Imam wake.

Na kama ikiwa Maamuma amemkuta Imam hajaanza hajakaribia wala hajaanza kurukuu basi hapa inambidi Maamuma kusoma Surat Al Fatiha kwa kadiri ya aya atakazoweza kuwahi kusoma katika kisomo chake hicho na sehemu itakayobakia ya Kisomo itakua imebebewa na kisomo cha Imam, na hii ndio hali pekee inayoruhusiwa Maamuma kukiruka kisomo cha Surat Al Fatiha Katika Sala kama iliyojadiliwa katika Bab Al Jumuah kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo Maamuma anamuwahi Imam katika kurukuu, basi hata kama Kisomo chake Maamuma cha Surat Al Fatiha hakijamalizika, basi Maamuma hua ni Masbuq basi ameiwahi Rakaa hio, kwani kama ikiwa Maamuma hakuwahi kurukuu pamoja na Imam, au akawa ni mwenye kurukuu lakini akawa ni mwenye kukosa utulivu ndani yake kutokana na kua alikua ni mwenye kung'ang'ania kutaka kumaliza kisomo cha Surat Al Fatiha na kisha akamkuta Imam ameshanyanyuka na yuko kwenye Itidal yaani kisimamo (na kama ikiwa amemkuta Imam anaelekea kwenye Sijda basi Sala ya Maamuma ambae ni Masbuq hua ni yenye kubatilika) basi Maamuma atakuaameikosa Rakaa hio na itambidi ailipe baada ya kumaliza Sala ya Jamaa.

Na inapotokea hali kama hii katika Rakaa yeyote ile pale inapokua Mtu anasali nyuma ya Imam, au inapotokea kua Mtu amechelewa na kuwahi kufunga Takbir basi Maamuma hutakwa kuchukua Tahadhari ya kuacha kusoma visomo vyote vinavyopendekezwa kusoma au au kufanya yale yanayopendekezwa kufanywa ndani ya Sala, na hivyo hua bora awe ni mwenye kuanza moja kwa moja kwenye kusoma Surat Al Fatiha ili asiikose Rakaa ya Jamaa husika.*(Imam Ibn Hajar Al Haythami katika Tuhfa)*

Ambapo kwa wale wenye hali ya Qudwa Haqqiqiyah ambayo hua ni hali ya kusali nyuma ya Imam ambae anasoma kwa kasi kubwa sana katika kisomo chake basi hua wanaruhusika kuchelewa katika hadi hatua tatu za Sala zao kutokana na kusoma Surat Al Fatiha, yaani wanaruhusiwa kuchelewa hadi kufikia kua Imam anaingia kwenye Sijda ya pili. Yaani hapa hua ni bila ya kuhesabu hatua za utulivu wa Imam baina ya kila hatua zake na hivyo kua ni takriban hatua Tano kama tukizijumuisha pamoja hatua za Utulivu baada ya Kunyanyuka kutoka kwenye Rukuu ya Imam na utuliuvu wa baina ya Sujud mibili za Imam.

Ambapo anasema Imam Ibn Al 'Imad, kuhusiana na Qawl Tamm kua ni jambo lililowazi kuaHatua za Nguzo tatu ndefu hua hazijumuishi Istiraha yaani kukaa kwa kupumziko baada ya Sujud ya pili kabla ya kusimama na wala hazijumuishi pumziko lolote laAttahiyat. Na hivyo kama Maamuma ambae ni Muwafiq aliemuwahi Imam wake ndani ya mipaka ya Viambatanisho hivi vya Sala vya hatua tatu ambazo ni ndefu basi atahesabika kua ameiwahi Rakaa husika. Ambapo hili huweza kutokea pale inapokua kuchelewa kwa Maamuma hakujafikia kwenye kuingia kwenye hatua Muhimu au Nguzo ya nne bado.

Ambapo hata hivyo, kama ikitokea hali ya kufanya hivyo, yaani kama hali ya kua, Imam tayari yuko katika Qiyam cha pili akiwa anasoma Surat AlFatiha, lakini Muwafiq akawa bado yuko katika kisimamo cha Kwanza akiwa anamalizia kisomo chaSurat AlFatiha yake, basi hapa moja kwa moja Sala ya Maamum itakua ni yenye kubatilika kama ikiwa hatafanya mojawapo kati ya mambo mawili yafuatayo:

(1) Maamumakuachana na kumalizia Kisomo cha Surat Al Fatiha yake na mara moja hapo hapo alipo aamue kumfuata Imam (ambapo kwa maana hio basi, Maamuma itambidi akirudie upya kisomo cha Surat AlFatiha yake kwa ajili ya rakaa yake hii mpya); na kisha baada ya Imam kumaliza na kutoa Salam, basi itambidi Maamuma asimame na kutekeleza rakaa iliyoikosa; au

(2) Maamuma kulazimika kuondoa Nia ya Sala ya Jamaa na kuachana na kumfuata Imam (yaani kua ni Mufaraqa) na hivyo kua ni mwenye kusali peke yake hadi mwisho ambapo katika hatua

hii basi itambidi awe ni mwenyekuendelea kuisoma Surat Al Fatiha yake na kuimalizia hadi mwisho, kwani akishindwa kuchukua hatua hii hadi katika kufikia kua Imam tayari ameshaingia kwenye Nguzo au Hatua ya nne wakati yeye Maamuma bado ameganda kwenye Hatua ya kwanza basi Sala ya Maamuma husika itakua ni yenye kubatilika. Ambapo hata hivyo hakutokua na madhara kama ikiwa hatua za Maamuma zitaambatana na za Imam kiasi ya kua wakati Maamuma atakapokua anarukuu basi na wakati huo huo Imam anahamia kweye hatua ya Kisimamo au Attahiyat.

Na hii ni kwa sababu katika Madhhab ya Imam Al Shafii kuna upendeleo maalum kwa ajili ya wasomaji wenyeupolepole wasiokua na kasi miongoni mwa Muwafiq na vilevile kwa Muwafiq wengine wenye visingizio vinavyokubalika, ambapo upendeleo huu hua ni kwa mujibu wa kanuni za kubakia nyuma kihatua Nyuma ya Imam kulingana na Maamua Masbuq hua kunahesabiwa kua ni tofauti.

Kutokana na kua na hadhi ya Msomaji asiekua na uwezo wa kusoma kwa kasi yaani anaesoma pole pole hua ni kubwa kuliko ya yule Mtu Masbuq aliechelewa na hivyo hua hahesabiki kua ameikosa Rakaa au ameibatilisha Sala yake, kwani hali ya Muwafiq hua ni kuhusiana na kuchelewa kutokana na kukosekana kwa uwezo wake kulingana na kasi ya Imam wakati hali ya Masbuq hua ni kuhusiana na kutowahi kuisoma na hivyo kukiwacha kisomo cha Surat Al Fatiha.

Na ndio maana kulingana na Hukmu ya nini cha kufanya katika wakati mtu anapokua ana Shaka ya kua ni Muwafiq ama Masbuq, basi bora mtu anatakiwa achague kuachana na kisomo cha Surat Al Fatiha ili kua ni mwenye kuhesabiwa kua ni mwenye kuchelewa nyuma ya Imam, kwani kuachana na kusoma Surat Al Fatiha hua ni kosa kubwa zaid kitofauti katika Sala, kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii.

Kwa maana hio basi Muwafiq mwenye udhuru unaokubalika kisharia yaani kama vile kutokua na kasi ya kusoma Surat Al Fatiha kutokana na kua hajuia Lugha ya Kiarabu vizuri, au ana matatizo megine ya kimaumbile yanayompelekea kua ni mwenye kuchelewa katika usomaji wake, na wala si kutokana na kua na matatizo ya wasi wasi wa kupita kiasi kwa mfano, hua ni mwenye kua na hadhi tofauti na Masbuq na hivyo hua hatakiwi kuiepuka Surat Al Fatiha na kurukuu pamoja na Imam, bali anatakiwa amalize kisomo chake hata kama itakua ni mwenye kuchelewa katika hatua zake Sala kulingana na hatua za Imam.

Ili kufahamiana zaidi kuhusiana na hali ya Muwafiq na Masbuq katika Sala basi na tuangalie mifano ya hali zinazoweza kutokea katika Sala ya Jamaa ambapo miongoni mwao ni pamoja na kwa mfano:

Tuseme kwa mfano kua Maamuma hamjui na wala hamfahamuImam, na hivyo alikuwa akitarajia na kumngojea Imam atulie (kwa kuwa si tu kwa sababu hajui nini cha kutarajia kutoka kwa Imam huyu, bali pia. alikusudia kufanya Mandub ya kucheleweshа kisomo cha Fatiha yake na kukusudia kusoma Fatiha wakati wa pumziko hilo au wakati wa kisomo cha Sura ya Imam), lakini ghafla Imam hasiti lakini akaingia kwenye rukuu badala yake (bila ya kusoma Sura yeyote baad ya Surat Al Fatiha, ambalo ni tukio lisilo tokea mara kwa mara lakini sasa hapa imeshatokea hivyo, au bada yake labda Imam ameamua kusoma Sura lakini ni Sura fupi Sana), na hivyo kumuachia Maamuma muda mfupi sana wa kumaliza Fatiha yake, na kisha baada ya hapo Imam anarukuu hapo hapo.

Hivyo Katika hali kama hii basi, Maamuma anachukuliwa kuwa na udhuru halali kama ule udhuru wa msomaji polepole tuliouangalia hapo kabla. Hilo inavyotakiwa ni kua, Maamumaanatakiwa amalizie Kisomo cha Surat Al Fatiha yake kama ilivyokua kwa msomaji pole pole, ila anatakiwa asome kwa haraka ili Maamuma asiwe ni mwenye kuchelewa ndani ya hatua za Nguzo tatu za Sala nyuma ya Imam, na hivyo katika kufanya kwake hivyo basi Maamuma atakua amefanikiwa kuiwahi Rakaa husika.Huu ni mfano wa Qudwa Hukmiyya.

Au pia kama Ikiwa Maamuma alikuwa akisoma Fatiha yake kwa Tartil [kwa usahihi na polepole; yaani kutamka kwa uwazi kila herufi, ambayo ni Sunna iliyothibiti] (wakati Imam hayupo), na Imamanarukuu kabla ya Maamum kumaliza Fatiha yake, na wakati huohuo kama Maamum kuisoma kwa haraka angeweza kumaliza kwa wakati kabla ya Imamhajarukuu, basi hukmu ya Maamuma huyu hua ni kama katika mfano hapo juu na msomaji mwepesi, kwa kuwa yeye pia ana udhuru halali wa kumaliza Fatiha. Huu ni mfano mwingine wa Qudwa Hukmiyya. *(Ibn Al 'Iwazimu, Qawl Tamm)*

Iwapo yale yaliyoelezwa katika mfano wa 1 na 2 yatatokea kwa Imam ambaye hafahamu hukumu za Madhhab ya Imam Al Shafii (na akashtushwa na hilo), basi lazima atambue kwamba hii ni halli inayoruhusiwa na Madhhab ya ImamA l Shafii. Kwa hakika jambo hili linapaswa kumfanya Imam afikirie kwa makini juu ya jambo hilo ili aweze kuona (kwa manufaa yake mwenyewe, kwa vile ni msimamo mkali zaidi na unatoka nje ya Wara') rehema ya kutoharakisha Qiyam chake na Salah yake, ima aisome vizuri. Tartil au kumpa Mfuasi wa Madhhab ya Shafii uhuru kwa kumstarehesha, au kumsomea Sura ndefu zaidi (lakini si lazima kuwa na Sura ndefu sana, kwani bado inapendekezwa kuweka tahfif katika kisomo ili iwe Sura kua kifupi yaani *takhfif Al qira'a.*

Na pia kwa mfano katika rakaa ya kwanza ya Imam, basi Maamuma alipoteza nafasi yake ya kumaliza kusoma Fatiha kabla ya Imam kurukuu, kwa sababu ya kujishughulisha na usomaji wa awali wa Mandub au kusikiliza kwa makini kisomo cha Imam chaSura inayofuatia wakati yeye mweneywe Maamuma bado hajasoma Sura Al Fatiha yake au labda alikua hafanyi chochote, hivyo katika hali hii, basi hua ni lazima kwa Maamuma kua amalize Kisomo cha Surat AlFatiha yake na pia atakua ana 'udhr wa kuchelewa katika hatua za Nguzo Tatu za Sala, kama ilivyo katika mifano miwili ya mwanzo ambapo hili ni jambo lililoelezewa wazi kwenye *Fath Al Mu'in* pale iliposema:

‘Muwafiq hua ameondolewa katika hali ya kua Masbuq, kwa maana hiyo basi, kama Maamuma Muwafiq hakumaliza kuisoma Surat Al Fatiha kwa sababu ya kujishughulisha na usomaji wa mwanzo ambao ni wenye hali ya kua ni Mandub, yaani kama vile dua ya ufunguzi, basi hata kama anafikiri kwamba hatoweza kuwahi kusoma Surat Al Fatiha pamoja na Imam katika kisimamo, basi katika hali kama hio, hua haipendekezwi tena kwa Maamuma kusoma kisomo cha awali cha Mandub, basi, anakuwa kama msomaji asiekua na kasi ya kusoma mwepesi na hivyo hapa itatumika sheria ya msomaji pole pole kwa ajili yake Maamuma huyu pia kama ilivyotajwa hapo awali, tena bila shaka bila khilaf yoyote katika Madhhab ya Imam Al Shafii.’(*Fath Al Mu'in***)**

Ambapo huu hua ni Mtizamo unaotegemewa yaani mtizamo wa *Al Qawl Al Mutammad wa Madhhab* ya Imam Al Shafii.

Na kama Maamuma akiwa ni Masbuq katika hali ya mazingira kama haya basi ingawa kwa kawaida Maamuma huyu hua ana haki ya kuiruka *Surat Al Fatiha* na kisha akarukuu pamoja na Imam, lakini katika wakati huu hua hawezi au haruhusiwi na hii ni kwa sababu Maamuma husika hua anahesabika kua ni Muqassir yaani mzembe, na hivyo itambidi kwa lazima kusoma *Surat Al Fatiha* kwa ukamilifu na kwa haraka kabla ya kumufata Imam ili kuzuia kubatilisha Sala yake.

Na hivyo Maamuma humbidi kuchagua baina ya kua Mufarraqa yaani kutofautiana na Imam wake au aende moja kwa moja kwenye hatua aliyokuwepo Imam ili kuzuia kubatilika kwa Sala yake, hivyo kama Imam atakua kwenye Itidal basi Maamuma itambidi kuachana na Rukuu yake na hivyo kupoteza Rakaa yake na hiyvo kama likitokea tukio la kwanza basi tunaona kua ile kusoma kwake Surat Al Fatiha ilikua ni bora kwake kwa ajili ya kutobatilisha Sala yake.

Mfano mwengine ni kua Kumekuwa na pendekezo kuhusu kusoma kila aya ya Surat Al Fatiha baada ya' kila aya aliyoisoma Imam ili Maamuma asikilize kisomo cha Imam huku akiwa ni mwenye kutimiza

sharti la Mam'uma la kusoma Fatiha. (na hili litamfanya Maamum kuwa huru kabisa kusikiliza Sura ya Imam kama Imam hatotulia baada ya kusoma Surat Al Fatiha). Ambapo juu ya hili hapa basi inabidi Mtu lazima ajue kua, hata hivyo, chaguo hili hua linatakiwa kua ni ni jambo lililofanywa kama suluhuisho la mwisho kabisa, kwa sababu bado inapendekezwa kwa Maamum kucheleweshe Fatiha mpaka Imam amalize kisomo cha Surat AlFatiha yake, hivyo kama ikiwa Maamuma hana sababu za msingi za kucheleweshe kisomochake cha Surat Al Fatiha yake mpaka baada ya kisomo cha Surat Al Fatiha cha kwani kufanya vyenginenevyo basi hupatikana na hali ya Khilaf Awla, ambapo hata hivyo hua hakuna ubaya kufanya kile kinachopendekezwa katika hili.

Hata hivyo kunaweza kuwepo na matatizo manne kutokana na pendekezo hili**: Ambayo ni kua kama Imam hatasimama katikati ya aya zake za kisomo cha Fatiha. Au**

Kusimama kwa Imam ni kufupi sana kwa Maamum kiasi kwamba hakutokuwepo uwezekano kwake wa kuweza kumaliza kusoma Aya fulani kabla ya Imam hajaanza aya inayofuata. au

Kwa sababu ya kutaka kwenda sambamba na Imam asiye wa kawaida, Maamum (hususanmsomaji taratibu) anaweza kuchanganyikiwa na hivyo kusahau ni aya gani au hata

Anaweza kupoteza Muwala [mwendelezo] wake katika wakati wa kusoma Surat Al Fatiha, ambapo hali hii kitatizo ha ndio mbaya zaidi kwani hua inambidi kurudia kisomo cha Surat Al Fatiha yake.

Ambapo Kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua, kusimamia Muwala ni sehemu muhimu ya kusoma Surat Al Fatiha. Ambapo Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanafafanua **'Muwala' kama 'kutamka kila neno bila kukatizwa kwa kutotenganisha kila neno kutoka kwa jengine kwa zaidi ya nafasi moja ya kupumua [Sakta Al Tanaffus; inayojulikana pia kama Sakta Al Istiraha au nafasi ya kupumzika; hii inatumika. kwa wale wasio na visingizio vyovyote halali vya kutulia kwa muda mrefu] au kugugumia [au mengine kama hayo, kwa wale walio na kisingizio halali cha kutulia kwa muda mrefu].**' *(Imam Al Bajuri, katika Hashiya yake)*

Hili linaweza kuleta matatizo iwapo Imam atasoma aya ya mwisho na ndefu zaidi ya Surat AlFatiha polepole, na kwa Tartil, kuanzia "SiraATalladhIna...", hadi mwisho (kumbuka kwamba kusimama kwenye "an'amta 'alayhim" ni Khilaf Awla. ; I'anat, 1:147), kwa mfano, kwa kuwa kuna uwezekano kwamba Sakta Al Istiraha ya Maamum inaweza kuwa ndefu kuliko inavyotakiwa, na hii itavunja Muwala.

Kwa sababu pendekezo hili linategemea tena mtindo wa usomaji wa Imam, linaweza kufanya kazi kwa baadhi tu na si kwa wengine. Kwa hiyo inahitaji kiwango fulani cha ushirikiano na maelewano baina ya Imam na Maamum kabla ya Sala; na kwa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, ushirikiano huo hua ni kwa namna ya pumziko anayotakiwa Imam kufanya kwa niaba ya Maamum.

Ama kuhusiana na aya ya Surat Al Aaraf isemayo kua:

﴿وَإِذَا قُرِئَ ٱلْقُرْءَانُ فَٱسْتَمِعُوا۟ لَهُۥ وَأَنصِتُوا۟ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾

Waidha Quria Al Qur'anu FaistamiaAu lahu Waansituu LaAalakum Turhamnuna.*(Surat Al Aaraf 7:204)*

Tafsir: **Hivyo Itakaposomwa Qur'an basi Isikilizeni na Kaeni Kimya ili mpate Kuingizwa kwenye Rehma.**

Basi kulingana na Wanazuoni wa Fiqh na Usuli wa Madahhab ya Imam Al Shafii wanasema kua neno Qur'an lililotumika kwenye Aya hii hua halikulenga kwenye Qur'an yenyewe kama Qur'an bali limelenga kwenye Khutba ya Ijumaa, kwa hio Maana halisi ya Aya hii ni kua:**'Wakati Khatib anaekhutubia Khutba ya Sala ya Ijumaa anapopanda kwenye Mimbar, basi msikilizeni kwa Makini na Nyamazeni kwa Utulivu ili mpate Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Ahl Ul Tafsir wa Tabiina akiwemo kina Imam Mujahid, Imam Said Ibn Jubayr na Imam Ataa Ibn Abi *Rabah Radhi Allahu Anhum'** *(Tafsir Lubab Al Tawil Fii Maani Al Tanzil)*

Kwani kwa maana hio basi Wanafiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii wamelitafsiri neno Qur'an lililotumika katika Aya hii kutoka kwenye asili yake.Ambapo neno Qur'an limetokana na neno Qaraa. Neno Qaraa hua linamaanisha Kusoma, Kusoma kitu kilichoandikwa, Kusoma Kitu bila ya kua nacho mikononi mwako au Mbele yako, Kufikisha Ujumbe, Kutoa Khutba, Kukusanya Pamoja, Kupanga kitu au vitu katika Mpangilio Maalum.Hivyo Qur'an imeitwa Qur'an kwa Sababu ni Kitabu Chenye Ujumbe unaotakiwa Kusomwa, Kutangaziwa, Kufikishwa, Kukusanywa pamoja na Kufanyiwa kazi.

Na kwa Maana hio basi Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni hua ni kua:**'Aya hii haina *Taaluq* yaani uhusiano wowote na usomaji wa Maamuma wa Surat Al Fatiha Nyuma ya Imam katika Sala. Na hivyo hata kama itakua na Uhusiano kama wanavyosema Wanazuoni wengine ambalo wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii hawalitii basi,Basi aya hii Itakua ndio sababu ya ziada inayofafanua kwanini Imam anatakiwa anyamaze kimya baada ya kusoma Surat Al Fatiha, yaani ili Maamuma nae apate kusoma Surat Al Fatiha yake. Na pia kwa Upande mwengine Basi Aya hii kama inazungumzia Qur'an basi inazungumzia Sura nyengine na wala si Surat Al Fatiha, na hii ni kwa sababu Aya hii inachukuliwa na Wanazuoni wa Usul kua ni aya yenye hali ya *Amm Makhsusi,au Amm Mutlaq* yaani aya ambayo ina ujumbe wenye hakika Usiobainishwa ndani yake.'**

Kwa sababu aya hii haijumuishi ndani yake Dalili ambayo inatakiwa kuwepo ili kuondoa Uwezekano wa kua kinachozungumziwa ndani yake kinaweza kikawa ni kitu kimoja kinachotokana na kitu chengine, na pia haijumuishi Dalili ya kua ni yenye kuondoa hali yake ya jumuisho lisilobainisha. Hivyo aya hii haina Dalili kua inazuia Usomwaji wa Surat Al Fatiha katika Sala nyuma ya Imam. Na hivyo haina Hukmu ya haramisho la kisomo cha Surat Al Fatiha ndani yake bali ndani yake ina hali ya jumlisho lenye Nasaha na Mafunzo ambayo yanaweza kutunufaisha ndani yake

Hivyo kutokana na kua ayah hii ina hali hio ya jumuisho lisilobainishwaikiwa na maana ya kua kwa wakati wowote na mahala popote itakaposomwa Qur'an watu wanyamaze, basi Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii wameifaham maana ya ayah hii ni yenye umaalum na isiyojumuisha hali ya jambo moja tu ambalo ni la kusoma Surat Al Fatiha katika Sala lililotolewa katika jumuisho hilo *na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mwenyewe kupitia katika Hadith ya Ubaidah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu*ambayo imethibitishwa usahihi wake na Wanazuoni mahiri wa Madhhab ya Imam Al Shafii kama Imam Al Bayhaqi na Imam Al Hakim na ndio msingi wa Hukmu yetu ambayo ni yenye kusema:

Amesema Ubaidah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Tulikua tunasali Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala ya Alfajir. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa anasoma Sura lakini ikawa vigumu kwake kusoma. Na baada ya kumaliza kusali, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza:'Inaonekana labda Mlikua mnasoma Nyuma ya Imam?'**

Ubayda Ibn Saamit *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: **'Sisi tukajibu Naam Ya Rasul Allah!'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema**: 'Msifanye hivyo isipokua kwa Ummu ul Quraan tu!Kwani Hakuna Sala kwa asieisoma Sura hio.'***(Imam Al Bukhari, Imam Abu Daud Imam At Tirmidhii, Imam An Nasai, Imam Ibn Khuzaymah, Imam Ibn Hibban, Imam Ad Daraqutni, Imam Al Hakim, Imam Al Bayhaqi na Imam Al Baghawi)*

Ambapo anasema Imam An Nawawi kua**: 'Suluhisho kuhusiana na Hadith mbali mbalizinazotumiwa na wale wanaohimiza kuacha usomaji wa Surat Al Fatiha, ni kua Hadith hizi zote ni dhaifu na hakuna hata moja miongoni mwao iliyothibitika usahih wake, kwani hakuna hata moja inayotoka moja kwa moja kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa sababu miongoni mwao kuna Hadith Mursal(upokezi wake umeishia kwa Tabiina) na *Mawquf*(imenasibishwa na Masahaba) na nyenginezo ni dhaifu au dhaifu sana'***(Al Majmuu)*

Labda na tuangalie baadhi ya mifano ya hadith hizo kwa kupitia ile hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Alahu Anhu* ambayo inasema kua: **'Wakati Imam anapofanya Takbir basi na wewe Maamuma unafanya Takibr pia, na anaposoma Qur'an basi nyamaza.'** *(Imam Ahmad, Imam Abu Daud, Imam Ibn Majah na Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo kutokana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam al Shafii na Imam Al Bayhaqi na Imam Abu Daud basi tunaon akua maneno yasemayo anaposoma Imam basi Nyamaza; yameongezwa na kuna utata juu ya nani aieyangeza maneno hayo.*(Imam Al Bayhaqi katika Awn Al Ma'abud)*

Ambapo sehemu ya maneno au ujumbe wa hadith hua yanajulikana kama Matn na hivyo kutokana na kua *Matn* ya hadith hii imeongezwa na kuipelekea hadithi hii kua na sifa ya *Mudraj* basi imekua haiwezi kutumika kama uthibitisho unaoweza kupinga hadith nyenginezo zinazotumika katika kutoa hukmu juu ya jambo hili, na hata hivyo kama hadith hii ingesahihishwa basi pia isingeweza kushinda hoja zilizizotumika katika kufafanua aya ya 204 ya Surat Al Araf tuliyoangalia hapo kabla na pia hadithi isemayo:

Anasema Ubaidah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Tulikua tunasali Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala ya Alfajir. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa anasoma Sura lakini ikawa vigumu kwake kusoma. Na baada ya kumaliza kusali, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* *akauliza*: Inaonekana labda Mlikua mnasoma Nyuma ya Imam?'**

Ubayda Ibn Saamit *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: **'Sisi tukajibu Naam Ya Rasul Allah!'**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema**: 'Msifanye hivyo isipokua kwa Surat Al Fatiha tu!Kwani Hakuna Sala kwa asieisoma Sura hio.'***(Sunnan Imam Abu Daud)*

Ambapo tunapoiangalia Hadithi ya Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Ahu* isemayo kua: '**Yeyote anayesali nyuma ya Imam, kisomo cha Imam ni kisomo chake'** *(Imam Al Daraqutni, Al Bayhaqi, na Ibn Abi Shayba.)*

Basi anasema Imam Al Sharqawi pamoja na Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii wengine, akiwemo ImamAl Nawawi, na Imam Al Ramli, ambao kwa kawaida huwa na mjadala wa Hadithi hii) kua Hadithi hii haijathibitishwa kwa uthabiti na imehesabiwa kua na ni dhaifu kwa mujibu wa Wanazuoni wa Hadith, kwa sababu ya baadhi ya matatizo katika Hadith yake. Na bila ya shaka Hadith dhaifi hua haziwezi kutumika katika mchanganuo wa kutafuta hukmu ya kutoa kuhuinana uharama na uhalali wa kitu.

Hivyo tuhitimishe kuhusiana na mtizamo huu wa juu ya kisomo cha Surat Al Fatiha Katika Sala kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii kwa kukumbushana kua:

(1) Kiwango cha chini cha hukm, kwa mujibu wa Madhhab ya Imam Al Shafii, ni kuwa ni Wajib kusoma Surat Al Fatiha nyuma ya Imam katika kila rakaa, na katika Sala zote, na huu ndio msimamo wa mwisho, unaotegemewa na ndio unaotakiwa kufuatwa, na ndio sahihi nahkuna mtizamo mwengine unaofaa zaidi ya huu kulingana na vithibitisho.

(2) Hukm iliyo bora, inayopatikana katika mjadala wetu wa Kayfiyya hapo juu, ni kwamba Imam anapaswa (yaani, Mandub na Sunna) asimame ili Maamuma wake wapatae kusoma na kumaliza kisomo cha Surat Al Fatiha zao. Na Kama Imam atashindwa kutekeleza jambo hilo basi haitokua dhambi kwake na wala haitoiathiri Sala kwa njia moja au nyengine na lakini kwa upande wa Maamuma basi itambidi nae kusoma Surat Al Fatiha yake wakati Imam anaposoma Sura nyengine baada ya kumaliza Surat Al Fatiha yake, au hata. wakati wa Fatiha ya Imam.

Naanasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya An Nawawi Al Shafii kua: 'Ama kwa Mtu anaefanya Ibada ya Sala na kisha akawa hakusoma Surat Al Fatiha katika Rakaa yake yeyote ile ndani yake, kutokana na kusahau na kisha akatoa Salam au akarukuu. Basi kuna Mitizamo miwili juu yake:

Ambapo Mtizamo wa Mwanzo ambao ndio Sahih na ndio Waliokubaliana Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kua:Mtu anaefanya Ibada ya Sala hana Kisingizio chochote cha kutotekeleza Wajibu wa Kusoma Surat Al Fatiha, Hivyo Mtu huyo akikumbuka tu kua hakusoma Surat Al Fatiha katika wakati ambao ameshaingia kwenye Rukuu au baada yake yaani kabla ya kunyanyuka kwa ajili ya kuingia kwenye kisimamo cha RakaaInayofuatia, basi Mtu huyo anatakiwa kwanza Arudi juu ili atimize Nguzo ya Kisomo cha Surat Al Fatiha na kisha aingie kwenye Rukuu.

Na Kama mtu atakua amekumbuka kua hakusoma Surat Al Fatiha katika Rakaa ya Kwanza wakati tahafi ameshaingia katika Rakaa ya pili,basi hapa Inambidi mtu huyo kutoihesabu Rakaa ya kwanza, na hivyo kisomo cha Surat Al Fatiha atakachosoma katika Raka hii ya Pili ndio kitaifanya Rakaa yake ya pili iwe ndio Rakaa ya Kwanza.

Na kama ikiwa mtu anaesali amekumbuka baada ya Kutoa Salam kua kumbe katika Rakaa moja hakusoma Surat Al Fatiha,basi itambidi mtu huyo hapo hapo kabla hajaondoka katika Sehemu ya kusalia asimame na kisha Asali kumalizia Rakaa moja na kisha afanye Sijdat As Sahw.

Na kama mtu huyo atakua amekumbuka wakati tayari ameshaondoka katika Sehemu aliyosalia basi Itambidi kuirudia Sala hio yote nzima *(Al Majmuu)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: **'Hairuhusiki kwa Maamuma kusoma Surat Al Fatiha pale anapokua Nyuma ya Imam iwe anasikiia na kusikikiza kisomo cha Imam Ama la.'**

Na anasemaSayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafikua:**'Kuna Mtizamo wa Imam Muhammad Ash Shaybani usemao kua: Inapendekezwa kwa Maamuma kusoma Surat Al Fatiha katika Sala ya Kimya na hii hua ni kwa ajili ya Hali kua na Tahadhari zaidi.'**

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua **Ni Makruh kwa Maamuma kusoma Surat Al Fatiha katika Sala nyuma ya Imam, iwe Imam huyo anasoma Surat Al Fatiha au Surat nyengine yeyote au amekaa kimya**. **Na vile vile wana mtizamo usemao kua: Inapendekezwa kwa Maamuma kusoma Surat Al Fatiha Kimya kimya Nyuma ya Imam lakini katika Sala za Kimya kimya na katika Rakaa ya tatu ya Sala ya Maghribi na pia katika Rakaa mbili za mwisho za Salat Al Ishaa Kwani Jukumu la Kisomo cha Maamuma hua linabebwa na Kisomo cha Imam.**

Ama kwa Upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: '**Kama Maamuma atakua hasikii Kisomo cha Imam basi Maamuma anaruhusika kusoma Surat Al Fatiha**. **Na hivyo inapendekezwa kusoma Surat Al Fatiha kwa Maamuma katika Sala za Kimya kimya, na pia pale tu Imam anapopimzika baada ya Surat Al Fatiha**, **Kwani Hairuhusiki kwa Maamuma Kusoma Kisomo chochote pale inapokua Imam yuko kwenye kisomo**. **Hivyo Kama Maamuma Hakusoma Surat Al Fatiha wakati akiwa anasali Nyuma ya Imam basi Sala yake haibatiliki, na hii ni kwa sababu Kisomo cha Imam hua kinamtosheleza Maamuma.'**

Ambapo ingawa huu pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal pia lakini hapo hapo Wanazuoni wa karibuni wa Madhhab hayo wenye Athari za Kisalafi wakiwemo kina Shaykh Ibn Baz na Shaykh Muhammad Al Uthaymin basi wamehamia kwenye Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na kuachana na Mtizamo Asilia wa Madhhab ya Imam Hanbal kwa kusema kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua hana Sala yule asiesoma Surat Al Fatiha'**(*Sahih Bukhari)*

Hivyo anasema Shaykh Ibn Baz kua: '**Hiki ndio kile kinachofanywa Na Imam pale anapotulia katika kusoma Surat Al Fatiha, au baada ya kusoma Surat Al Fatiha au kabla ya Kusoma Sura nyengine**. **Ambapo hata kama Imam hakusita basi yule anaesali Nyuma yakr anatakiwa asome Surat Al Fatiha yake hata kama Imam atakua anendelea na kusoma Sura nyengine.'**

Na pia liliulizwa Baraza kuu la Kiislam Duniani la Kamati ya Fatwa linalojulikana pia kama *Rabita Al Aalam Islamiya yenye* Makao Makuu yake ncbini Sauda Arabia inayojumuisha Wanazuoni wakubwa wa Fiqh wa Madhhab Mbali mbali ambayo ndio Iliyotoa Fatwa ya Muandamo ya mwezi ya maaka 1986 kua Kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua Kila sehemu ina Muonekano wa Muandamo wake

Na hivyo Baraza la Kamati hio yalilipouziwa kuhusiana na Surat Al Fatiha katika Sala basi likatoa Fatwa isemayo kua: '**Mtizamo Sahih wa Wanazuoni hua ni kua Ni Wajib kusoma Surat Al Fatiha katika Sala pale Mtu anaposali peke yake na pia pale Mtu anapokua Imam na pia kwa Maamuma wake, iwe kwenye Sala ya Sauti au Sala ya Kimya kimya**. **Na hii ni kutokana na Usahihi wa vithibitisho vya Maandiko.'**

Ama kuhusiana na Maana ya maneno ya Aya isemayo

﴿وَإِذَا قُرِئَ ٱلْقُرْءَانُ فَٱسْتَمِعُوا۟ لَهُۥ وَأَنصِتُوا۟ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾

Waidha Quria Al Qur'anu FaistamiaAu lahu Waansituu LaAalakum Turhamnuna. *(Surat Al Aaraf 7:204)*

Tafsir: **Hivyo Itakaposomwa Qur'an basi Isikilizeni na Kaeni Kimya ili mpate Kuingizwa kwenye Rehma.**

Basi Aya hii imebeba Maana ya Jumuisho la Ujumla ambalo pia ndio lile lililobebwa na maana ya Hadith isemayo kua; Amesema Rasul Allah Salallhu Alayhi wa Salam kua inaposomaa Qur'an basi isikilizeni kwa Umakini. **Na hivyo basi Jumuisho hili hua linabeba amrisho la Kisomo cha Qur'an kwa ujumla, iwe Surat Al Fatiha ama Sura nyengine yeyote ile ndani ya Qur'an.**

Hivyo maandiko mawili haya ya Aya na Hadith yanabeba Ujumbe wa Hukm ya amrisho la Kiujumla.Ambapo hapo hapo kuna Hukmu nyengine ya Amrisho jengine Makhsus au Maalum kwa ajili ya Surat Al Fatiha lisemaloKua: "Hakuna Sala kwa asiesoma Surat Al Fatiha" na hivyo kutokana na amrisho hili la hadith hii basi tunaona kua lile amrisho la hadith isemayo kua:Kisomo cha Imam Kinamtosheleza Na anaesali Nyuma yake" kua ni Dhaifu.

Na hivyo hua si sahih kusema kua Kiitikio cha Aamin cha wote katika Sala hua kinachukua nafasi ya Kisomo cha Surat Al Fatiha.Na hivyo basi kutofautiana kwa Wanazuoni juu ya Jambo hili kusichukuliwe kua ndio sababu ya **Waislam kuchukiana na kusababisha Ufa ktika Jamii ya Kiislam, kupeana migongo baina yetu miongoni mwetubali tofauti hizi zichukuliwe kua ndio sababu ya Kuendelea kusoma na kulifuatilia kwa kina zaidi jambo hili ili kujua zaid juu yake.**

Kwani hivyo ndivyo yalivyo malengo ya Hukmu na Sharia za Dini ya Kiislam ambayo ni kusimamia Maslahi ya Uiislam katika Kujenga Umoja wa Jamii ya Kiislam kwa Ujumla na wala si kusababisha Ufa katika Jamii.

KUSOMAQUR'AN KWA KUTUMIA MSAHAFU NDANI YA SALA.

❖❖❖

Tumeona namna ilivyo Mitizamo ya Wanazuoni kuhusiana na Umuhimu wa Kusoma Surat Al Fatiha kaa kila Anesali, Anaesalisha na anaesalishwa kulingana na Madhhab tofauti.Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tumeona kua Surat Al Fatiha ni lazima isomwe katika Kila Rakaa na kama hakufanya hivyo basi Sala yake itakua ni Batili.Kwa sababu Surat Al Fatiha ndio nguzo ya Sala na ndio Sala yenyewe.

Sasa kuna suali ambalo inabdi tujiulize ambalo ni kua Tuseme kua Mtu ndio kwanza amesilimu na Hajui kusoma Qur'an jee atatekelezaje Nguzo hii ya Kisomo cha Surat Al Fatiha?

Au Labda tuseme kua Mtu husika ni Muislam lakini kwa bahati mbaya hakuwahi kujifunza kusoma Qur'an kutokana na sababu mbali mbali, lakini sasa umefikia wakati ameamua kurudi kwa Mola wake na anajifunza Kusali. Jee Atasali vipi?

Hivyo jibu la Suali hili linapatikana kwenye Hadith ya Abd Allah Ibn Abi Awfa *Radhi Allahu Anhu* ambae anasema kua**: 'Kuna mtu alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na akasema: Ya *Rasul Allah* hebu nifundishe mimi Maneno ya sehemu ya Qur'an yatakayo nitosheleza kwa sababu mimi sijui kusoma.**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *kumwambia Mtu huyo kua: '**Sema:**

سبحان الله والحمد لله ، ولا إله إلا الله ، والله أكبر ، ولا حول ولا قوة إلا بالله.

Subhanah Allah, wa Alhamd lillah wa La Ilaha Illa Allah wa Allahu Akbar wa la Quwwata Illa bi Allah **- Utukufu ni wa Allah pekee, na Shukrani zote ni za Allah, Na hakuna Ma anaestahiki Kuabudiwa isipokua Allah na Allah ndie Mkubwa kuliko kitu chochote na hakuna Nguvu wala uwezo isipokua kutoka kwa Allah.'**

Hivyo Mtu huyo akafunga mkono wake ngumi (kuashiria kua ametamkononi kitu chenye maana sana) huku akionesha kua amejawa na furaha ya kunufaika na mambo mengi sana na kisha akasema: 'Haya Maneno ni kwa Ajili ya Mola wangu, hivyo Jee mimi nitapata yepi?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akamwambia kua Sema:**

اللهم اغفرلى و ارحمنى وحدنى وارزكنى وعفنى

Allahuma Ighfir li wa Arhamni Wahdini wa Rzuqni wa Aafini **- Ya Allah Nisamehe, na Uniingize kwenye Rehma na uniongoze na Uniruzuku na Unijaalie Afya njema.**

Ambapo Bwana huyo akafunga mkono wake mwengine kwa furaha kama alivyofanya mwanzo na kisha akanyanyuka na kuondoka*(Sunan An Nasai, Sunan Abu Daud)*

Na bila ya shaka Wanazuoni wanakubaliana kua kulingana na Hadith hii basi ni kua Kama Mtu hajui kusoma Surat Al Fatiha, basi anaweza kusoma Dhikr zilizotajwa kwenye Hadith hii.

Na kama mtu anajua labda tuseme Aya mbili Tatu tu za Surat Al Fatiha basi anatakiwa asome Aya hizo hizo azijuazo hadi atakapojua. Hivyo anaweza akasema *Bismi Allahi Rahmani Rahiim Alhamd Lillahi Rabbi Al Alamiin* kama hayo ndio ayajuao kwani amesema pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**'Mtu anatakiwa asome kile anachokijua katika Qur'an na kama hajui basi afanye Dhikr Allah na Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'***(Imam Abu Daud)*

Na aliulizwa Imam Al Zuhri ambapo nae akasema: **'Wetu wema miongoni mwa watu wetu walikua wakisali huku wakisoma kutoka kwenye Msahafu' na hii ni kutokana na Mtizamo wa Ataa, na Yahya Al Ansari kupitia kwa Al Hasan na Muhamamad kuhusiana na Sala za Sunna na hua inaruhusika kusoma kutoka kwenye Msahaafu.'**

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanasema kuhusiana na suali hili kua: **'Kama Mtu anajua kusoma ila hajahifadhi basi hua anaruhusika pia Kuchukua Kartasi na kuandika Surat Al Fatiha na kisha akaisoma katika wakati wa Kusali, au anaruhusika pia kuchukua Juzuu akasoma pia.Au inakubalika pia kwa Mtu kumsalisha Mtu asiejua Kusali kwa kumsomea Surat Al Fatiha kwa sauti ili Maamuma huyo asiejua afuate kisomo hicho.Na pia kama hakuna njia nyengine basi Mtu anatakiwa Asali kwa kufuata Vitendo vya Imam tu hadi atakapojua.***(Al Majmuu, Nihayat Al Muhtaj, Al Mutammad Fi Fiqh Al Shafii)*

Kwani Anasema pia Shaykh Ul Islami Imam Al Shafii Al Saghir Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Ramli Al Shafii kua: '**Kama Mtu hajui Kusoma Surat Al Fatiha, na hakuwahi kujifunza labda kwa kutokuwepo Mda wa Kutosha, au kutokana na Uzito wa Ufaham na hawezi pia kuisoma kutoka kwenye Msahafu basi Mtu huyo itambidi achukue hatua Mbadala.***'(Nihaya Al Muhtaj)*

Ambapo tunaoaingalia Fatwa hii ya Imam Al Ramli ndani yake imezungumzia mambo mawiliAmbapo kwanza ni kuruhusika Kwa Mtu Kusali huku akiwa ameshika Mas-haf na kusoma Qur'an kutokana nayo.

Ambapo hili ni Jambo ambalo wengi wetu wamekua wakijiuliza Juu yake, hususan katika kipindi kama hiki kwa Ile Miskiti yenye Kusoma Juzuu nzima kila siku katika Salat At Tarweh, pale inapokua Imam husika hajahifadhi Sura husika.

Na kisha pia Fatwa yetu inazungumzia kutumia kwa Njia Mbadala pale inapokua hakuna njia nyengine yeyete ya Mtu kua na uwezo wa Kusoma Qur'an katika wakati husika. Ambapo tunapozungumzia Njia Mbadala basi miongoni mwao hua ni zile tulizozitaja hapo kabla yaani kama alivyoamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Mtu na aseme:

سبحان الله والحمد لله ، ولا إله إلا الله ، والله أكبر ، ولا حول ولا قوة إلا بالله.

***Subhanah Allah, wa Alhamd lillah wa La Ilaha Illa Allah wa Allahu Akbar wa la Quwwata Illa bi Allah* - Utukufu ni wa Allah pekee, na Shukrani zote ni za Allah, Na hakuna Ma anaestahiki Kuabudiwa isipokua Allah na Allah ndie Mkubwa kuliko kitu chochote na hakuna Nguvu wala uwezo isipokua kutoka kwa Allah.'**

Au inakubalika pia kwa Mtu kumsalisha Mtu asiejua Kusali kwa kumsomea Surat Al Fatiha Sauti ili Maamuma huyo asiejua afuate kisomo hicho.

Au inakubalika pia kwa Mtu asiekuakatika Sala kukaa pembeni yake na kumsomea Surat AlFatiha Mtu huyo asiejua nae akaifuata inavyosomwa wakati yeye akiwa ndani ya Sala.

Na pia kama hakuna njia nyengine basi Mtu anatakiwa Asali kwa kufuata Vitendo vya Imam tu hadi atakapojua.

Kwani hapa inabidi tufahamishane kua Kila Muislam anatakiwa aijue Surat Al Fatiha kwani ndio Sala yenyewe kama tulivyosema.Lakini sasa kama tulivyoona pia si kila Muislam hua ni mwenye kujiua Surat Al Fatiha na hii ni kwa sababu tofauti mbali mbali.

Na hata kwa hao wanaosema kua Wanaijua basi nao unaweza kukuta kua katika watu Kumi basi watatu kati yao wanaisoma kwa Makosa. Wakati tunapozungumzia kuhusiana na Surat Al Fatiha basi kama Mtu akiisoma na akakosea na akajua kua Kimaana amekosea na kisha akawa hakuirudia basi Sala ya Mtu husika hua ni Batili.Lakini kama mtu akiisoma na kisha akakosea kutamka lakini hakujua kua amekosea basi Sala yake hua ni Sahih.

Ambapo anasema Imam Muhammad Wahba Al Zuhayl kua: '**Kuna umuhimu mkubwa sana wa kua na umakini katika usomaji kwa sababu utakapobadilisha usomaji wa maneno ya aya utakua umebadilisha maana ya aya, hivyo kama mtu akibadilisha kwa makusudi basi hua amebadilisha maana na amebatiisha Sala yake, lakini ikiwa kwa bahati mbaya,basi itambidi mtu huyo kurudia tena aya hio, kwani kufanya makosa kwa bahati mbaya kwenye kisomo cha ndaniya Sala hua hakubatilishi Sala.'***(Al Mutammad)*

Ambapo anasema Imam Abu Muhammad Dhiau Ad Din Abd Al Malik Ibn Yusuf Al Juwayn Al Shafii Al Haramayn kua: '**Hua hakuna Tatizo kuirudia Surat Al Fatiha kama ikiwa mtu anadhani kua labda amekosea namna alivyoisoma aya, kwa sababu mtu hua anasamehewa utokanana kukosea kwake, na pia hata kama akiirudia aya au neno lake bila ya kua na sababu yeyote ya msingi.'**

Kwani amesema ***Aisha Radhi Allahu Anha*** kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Kua: 'Yule mwenye ujuzi wa kusoma Qur'an atafufuliwa na kua pamoja na Malaika watiifu na Yule anaesoma Qur'an na kisha akawa anapata ugumu katika kusoma kwake basi atalipwa mara mbili''***(Imam Muslim)*

Na akasema Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua**: 'Mtu anaepata tabu katika kusoma kisomo cha Qur'an hua ni Yule anaedodosa katika kisomo chake kutokana na kutoweza kuihifadhi vizuri, atakua na malipo mara mbili, kwanza atakua na malipo ya kuisoma Qur'an na kisha atalipwa malipo ya jitihada zake katika kuisoma.'**

Hivyo ni Wajibu wetu Waislam kwa kila asieijua basi ajijtahid kuhakikisha kua anaijua kwani kwa kila asieijua basi anatakiwa aijue.Kwani anasema Imam Said Ibn Muhammad Baali Baeshen Al Duani Al Hadhrami Al Shafii kua:**'Nguzo ya Nne ya Sala ni Kisomo cha Surat Al Fatiha, katika wakati wa Kisimamo cha Baina ya Kila Rakaa katika Sala zote za Fardhi na Sunna, kwa Mtu anaesali peke yake au Jamaa, Kwa Sala za Sauti ama za Kimya kimya, ni Lazima Kuisoma Surat Al Fatiha iwe kutoka kwenye Ufahamu wake, Kwa Kufahamishwa na akafuata au kwa Kusoma kutoka kwenye Mas-haf'** *(Bushra Al Karim bi Sharh Masail Tarim - Sharh Al Muqaddima Al Hadhramiya)*

Kwani amesema Imam Abd Allah Ibn Abi Mulaykah Al Makhzumi kua: '**Aisha *Radhi Allahu Anha* alikua akiongozwa na Mfanyakazi wake aitwae Dhakwan kwenye Sala hukua kiwa ameshika Mas-haf.'***(Imam Abu Daud - Kitab Al Masahif)*

Naam Imam Ibn Abi Mulaykah ni Imam Mcha Mungu ambae alisoma kwa Masahaba wafikao 30 kama anavyosema mwenyewe kua: **'Mimi nimekutana na Masahaba 30 wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam ambapo kila mmoja wao alikua akiuogopa Unafiq, kwani hakuna hata mmoja wao aliekua akidai kua ana Imani kubwa sana kama ya Jibril au Mikail'***(Sahih Bukhari)*

Ambapo Masahaba aliokutana nao ni pamoja na Ali Ibn Abi Talib, Saad Ibn Abi Waqqas, Aisha, Asma, Ummu Salamah,Abd Allah Ibn Masud, Abd Allah Ibn Umar, Abd Allah Ibn Abbas, Abd Allah Ibn Zubayr, Abu Hurayrah, Uqbah, Miswar na wengineo *Radhi Allahu Anhum.*

Na nimemuelezea kidogo Imam Ibn Mulaykah kwa sababu ya Kauli yake kuhusiana Na Sala ya *Aisha Radhi Allahu Anha* aliyokua akisalishwa na Imam ambae alikua akisoma kutoka kwenye Masahafu, Imam ambae ni Mfanyakazi wake. Hivyo kauli hii ya Imam Ibn Abi Mulaykah ndio miongoni mwa Vithibitisho wanavyotumia Wanazuoni juu ya kuruhusika kwa Mtu anaesali kusoma kutoka kwenye Msahafu.

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Al Hafidh Abu Fadhl Ibn Hajar Al Asqallani kua: '**Ruhusa ya mtu kusoma kutoka kwenye Msahafu imechukuliwa kutoka kwenye Hadith hii Ambapo hapo hapo kuna Wanazuoni ambao wamekataza Kusali huku mtu akiwa ameshika Msahafu kwa sababu hua inajumuisha kaa mtu kua ni mwenye kufanya vitendo vingi vya ziada visivyostahiki ndani ya Sala.'**

Na hapa inabidi turudi tena kwa Imam wetu Shaykh Ul Islami Imam Al Shafii Al Saghir Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Ramli Al Shafii ambae yeye anasema kua**: 'Sala hua inabatilika pale inapokua ndani yake kufanya vitendo vingi vya ziada ndani yake. Hivyo hua inaruhusika kufanya baadhi ya vitendo kidogo kwa mfano pale Mtu anapokua anasali kisha akamuona Nge, na akanuia Kumuua, n.k hivyo kuna yanayoruhusiwa na yasiyoruhusiwa. Hivyo Kama mtu atafungua Msahafu na kisha Akazingatia kile kinachosomwa, au yeye mwenyewe akasoma ndani ya Msahafu huo, na hata kama atafungua ukurasa mwengine basi hatokua ni**

mwenye Kuibatilisha Sala yake na hii ni kwa sababu kitendo hicho hakihesabiki kua ni Miongoni mwa vitendo vingi vya ziada.'*(Nihayat Al Muhtaj)*

Na anasema Imam Ala Ad Din Al Kasani Al Hanafi kua: **'Kulingana na mtizamo wa Imam Abu Hanifa basi Mtu akisali na kusoma kutoka kwenye Msahafu basi Sala yake hubatilika Lakini kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Yusuf na Imam Ash Shaybani (Wanafunzi wa Imam Abu Hanifa) basi Sala ya Mtu husika haibatiliki. Lakini hata hivyo kwa upande wa Mtizamo huo wa Imam Abu Yusuf na Imam Muhammad Ash Shaybani wanasema kua inaruhusika na hii ni kwa sababu kusoma Qur'an kutoka kwenye Msahafu hua ni Ibada Lakini hata hivyo hua haipendeezwi kwa sababu ya kua kufanya hivyo hua ni kama kuwaiga watu wa Ahl Al Kitab.'**

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Hanbal basi Sala haibatiliki kwa Kusoma kutoka kwenye Msahafu na kuna kauli moja pia kutoka kwa Malik.*(Umdat Al Qarri)*

Tunaporudi kwa upande wa Imam Abu Hanifa basi Wanazuoni wa Madhhab yake wameifafanua Hadith hii kulingana na utetezi wa mtizamo wao kwa kusema kua: 'Dhakwan alikua amehifadhi baaadhi tu ya sehemu ya Sura za Qur'an wakati sharti la kusoma kutoka kwenye Msahafu kulingana n Madhhab ya Imam Abu Hanifa ni kua: '**Yule anaesoma anatakiwa awe si yule ambae amehifadhi kile anachotaka kukisoma ndani ya Sala. Kama vile ambavyo ilivyokua kwa upande wa Dhakwan ambako hakukutokana na kutiwa ari katika kufanya hivyo bali kulitokana na ufahamu wake, na hivo alikua akiuwacha msahafu wazi kwa ajili ya maneno mawili matatu ambayo hayabatilishi Sala.''** .*(Ila Al Sunnah)*

Ambapo kwa mtizamo wa Imam Badr Al Ayni basi tunaona ni kua**: 'Dhakwan alikua akisoma nkuhifadhi sehemu za Qur'an kabla ya hata hajaingia ndanya Sala. Na kisha baada ya hapo husimama na kusimamisha Sala na kuanza kusoma kile alichokihifadhi.'***(Al Binaya fi sharh Al Hidaya 2/427)*

Lakinikwa upande wa Imam Al Kasani basi yeye anasema kua: **'Kuna uwezekano wa kua Habari mbil hizi zinaelezea mambo mawli tofaut yaani Dhakwan alikua akisalisha akiwa anasoma kwenye msahafu na pia alikua akisoma kutoka kwenye msahafu wkat anapokua nje ya sala.'** *(Bada'i Al Sana'i 1/236)*

Hivyo na tumalizie na Kauli ya *Shaykh Ul Islami* Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi ambae anasema kua: '**Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Hanbal basi inaruhusikakusoma kutoka kwenye Msahafu iwe kwenye Sala za Fardhi au za Sunna iwe mtu amehifadhi anachokisoma ama la Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao Wanaruhusu kusoma kutoka kwenye msahafu pale mtu anapokua kwenye Sala za Sunna na Taraweh tu.'***(Al Majmuu Imam An Nawawi)*

Kwani miongoni mwa vithibitiaho vya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa juu ya kutokukubalika kusali huku ukiwa unasoma kwenye Msahafu ni ile hadith isemayo:

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ حُجْرٍ، أَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ جَعْفَرٍ، عَنْ يَحْيَى بْنِ عَلِيِّ بْنِ يَحْيَى بْنِ خَلاَّدِ بْنِ رَافِعٍ الزُّرَقِيِّ، عَنْ جَدِّهِ، عَنْ رِفَاعَةَ بْنِ رَافِعٍ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم بَيْنَمَا هُوَ جَالِسٌ فِي

الْمَسْجِدِ يَوْمًا قَالَ رِفَاعَةُ وَنَحْنُ مَعَهُ إِذْ جَاءَهُ رَجُلٌ كَالْبَدَوِيِّ فَصَلَّى فَأَخَفَّ صَلاَتَهُ ثُمَّ انْصَرَفَ فَسَلَّمَ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَقَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَرَجَعَ فَصَلَّى ثُمَّ جَاءَ فَسَلَّمَ عَلَيْهِ فَقَالَ " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَفَعَلَ ذَلِكَ مَرَّتَيْنِ أَوْ ثَلاَثًا كُلُّ ذَلِكَ يَأْتِي النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم فَيُسَلِّمُ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَيَقُولُ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَخَافَ النَّاسُ وَكَبُرَ عَلَيْهِمْ أَنْ يَكُونَ مَنْ أَخَفَّ صَلاَتَهُ لَمْ يُصَلِّ فَقَالَ الرَّجُلُ فِي آخِرِ ذَلِكَ فَأَرِنِي وَعَلِّمْنِي فَإِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ أُصِيبُ وَأُخْطِئُ . فَقَالَ " أَجَلْ إِذَا قُمْتَ إِلَى الصَّلاَةِ فَتَوَضَّأْ كَمَا أَمَرَكَ اللَّهُ ثُمَّ تَشَهَّدْ وَأَقِمْ فَإِنْ كَانَ مَعَكَ قُرْآنٌ فَاقْرَأْ وَإِلاَّ فَاحْمَدِ اللَّهَ وَكَبِّرْهُ وَهَلِّلْهُ ثُمَّ ارْكَعْ فَاطْمَئِنَّ رَاكِعًا ثُمَّ اعْتَدِلْ قَائِمًا ثُمَّ اسْجُدْ فَاعْتَدِلْ سَاجِدًا ثُمَّ اجْلِسْ فَاطْمَئِنَّ جَالِسًا ثُمَّ قُمْ فَإِذَا فَعَلْتَ ذَلِكَ فَقَدْ تَمَّتْ صَلاَتُكَ وَإِنِ انْتَقَصْتَ مِنْهُ شَيْئًا انْتَقَصْتَ مِنْ صَلاَتِكَ " . قَالَ وَكَانَ هَذَا أَهْوَنَ عَلَيْهِمْ مِنَ الأَوَّلِ أَنَّهُ مَنِ انْتَقَصَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا انْتَقَصَ مِنْ صَلاَتِهِ وَلَمْ تَذْهَبْ كُلُّهَا . قَالَ وَفِي الْبَابِ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ وَعَمَّارِ بْنِ يَاسِرٍ . قَالَ أَبُو عِيسَى حَدِيثُ رِفَاعَةَ بْنِ رَافِعٍ حَدِيثٌ حَسَنٌ . وَقَدْ رُوِيَ عَنْ رِفَاعَةَ هَذَا الْحَدِيثُ مِنْ غَيْرِ وَجْهٍ.

Amesema Rifaa Ibn Rafii *Radhi Allahu Anhu* kua, Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua amekaa Msikitini nasi tukiwa pamoja nae.

Na mara akaingia Bedui alieonekana kama kwamba anataka Kusali, na Kasali Sala yake kwa Ufupi sana, na kisha alipomaliza akanyanyuka na kumsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akitikia *Wa Alaykum Salaam* na kisha akasema: 'Rudi ukasali tena, kwani kwa hakika wewe Hujasali.'**

Hivyo yule Bedui akarudia Kusali kisha akamsalimia tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akamuitikia na kisha akamwambia Rudia tena kusali kwani kwa hakika wewe hukusali.

Bedui akarudia Kusali na kurudishwa kama mara mbili tatu na kila mara *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anamwambia Arudie kusali.

Tukio hili liliwashtua Sana Masahaba kutokana na kuona kua kumbe Mtu anaesali Sala fupi hua hana sala.

Lakini mwishowe Bedui huyo akasema: 'Ya Rasul Allah, basi bora nifundishe kwani mimi ni Ibn Adam mwenye kujihangaisha na kukosea.'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: Sawa Unapotaka kusali tia Udhu kama alivyokuamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kisha Adhini na Kimu Sala pia.**

Kisha Ukisali basi Soma Qur'an kama unajua na kama hujui basi Mtukuze *Allah Subhanah wa Ta'ala,* fanya Dhikr Allah na fanya Tahlil,Kisha Rukuu hadi uwe umetulia kwenye Rukuu yako, kisha Simama Sawia,kisha Sujudu kikamilifu, kisha Kaa kitako hadi uhakikishe kua umepumzika,kisha Sujudu kikamilifu,Kisha Simama na ukifanya hivyo utakua umekamilisha Sala yako, na ukipunguza basi utakua hukuikamilisha Sala yako.

Na Hivyo hua ni bora kuliko kutokamilisha, kwani ikipungua kitu Sala yako basi itakupunguzia Malipo yake lakini hutokosa kabisa.

Hili lilikuwa jepesi kwao kuliko lile la kwanza, kwa sababu mwenye kujiepusha na jambo hilo ameipunguzia Sala yake, lakini hakuikosa Yote. Ambapo amesema Abu Hurairah na Ammar Ibn Yassir, Abu Issa amesema: "Hadithi ya Rifa'ah Ibn Rafi' ni hadithi nzuri." Imepokewa kuhusiana na Ubora wa Hadithi hii kua ni Hadith isiyokua na Shaka.*(Sunan At Tirmidhii)***

Ambapo hii ni Hadith Sahih na wafuasi wa Imam Abu Hanifa wanasema kua: '**Hadith hii haikusema kua asiejua kusoma Qur'an basi achukue Msahafu asome bali imesema kua anatakiwa Amtukuze Allah badala yake'**

Ambapo anasema Al Qadhi Al Qudhat Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basri Al Shafii kua: '**Jukumu La Imam hua ni Kulinda na Kusimamia Usimamizi wa Sharia na Qanuni za Dini ya Kiislam.'**

Na kisha anasema katika kitabu chake *Al Hawi Al Kabir Fii Fiqh Madhhab Al Shafii* kua : '**Inaruhusika kwa Mtu kusoma kutoka katika Msahafu huku akiwa anasali, na wala Sala yake haitobatilika.**

Na ingawa Abu Hanifa anachukulia kua Sala ya Mtu afanyae hivyo itakua imebatilika kutokana na kitendo chake cha kufungua Kurasa za Msahafu kua ni chenye wingi wa ziada kivitendo.

Ambapo hili si jambo Sahih, kwani ukweli ni kua sababu ya kubatilika kwa Sala kwa Mtu kama huyu anaesoma Msahafu katika kisomo cha Qur'an cha ndani ya Sala hua ni aidha Katika Kuangalia Msahafu au Kufungua Kurasa za Msahafu. Na sisi tunajua kua Kuangalia Msahafu hakubatilishi Sala, kwani Mtu anaesali na Mbele yake ukawepo Msahafu na akauangalia basi habatilishi Sala yake kutokana na kitendo hicho.

Ama tukizungumzia kuhusiana na kitendo cha kubadilisha Kurasa za Msahafu katika kuzifungua kwake katika wakati wa kusoma basi hakitokua ni kitendo chenye uziada na hii ni kwa sababu kufungua kwake huko Kurasa za Msahafu hua ni baada ya mda na wala si hapo kwa hapo.

Kwa Maana hio basi Sala ya Mtu anaesali huku akiwa anasoma Qur'an kutoka katika Msahafu hua haibatiliki.'

Kwani huyo ni Imam Al Mawardi Al Shafii ambae ni Mwanafiqh na ndie Baba wa ilm ya Mamlaka na Utawala katika Uislam na haishangazi kua darja yake watika wakati wa Uhai wake ilikua ni Qadhi Al Qudhat yaani Qadhi wa Maqadhi Na mbalia ya Al hawi al Kabir lakini pia miongoni mwa vitabu vyake ni pamoja na Ahkam Al Sultaniya, Nasihat Al Muluk, Qawanin Al Wazarat n.k.

Na Mtizamo huo wa Qadhi Al Qudhat Imam Al Mawardi kuhusiana na kusoma kutoka katika Msahafu kwa mtu anaesali hakubatilishi Sala yake ndio pia Mtizamo ulioelezewa na Imam Shams Ad Din Wawili ambao ni Imam Al Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Ramli na pia na Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini katika vitabu vyao vya *Nihayat Al Muhtaj na Al Mughni Al Muhtaj.*

Ama kuhusiana na kusoma Qur'an kutoka katika simu pale inapokua mtu husika hana msahafu basi, basi hua kunafaa na kunakubalika pia na malipo yake hua ni kutokana na kuangalia maneno ya Qur'an ambayo ingawa hua ni tofauti na maneno yaliyomo ndani ya Msahafu kwani hua yanatoweka, kwa sabau

ni ya ki elektroniki lakini malipo yake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni sawia kutokanana utukufu wa asili wa maneno ya Qur'an.

Na hii hua ni kulingana na hali ya mazingira ilivyo kwani katika kipindi cha *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* ilikua hakuna kartasi na hivyo Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua wakitumia Ngozi, Vipande vya Mbao, Magome ya Mti, Mawe n.k kwa ajili ya kuiandika na kuisoma pia, hivyo kitu chochote kile chenye kubeba maneno matukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* nacho hua ni chenye kua na utukufu, nakueshimiwa kutokana na utukufu wa Qur'an.

KUITIKIA AMIIN BAADA YA KISOMO CHA SURAT AL FATIHA

❖❖❖

Neno Aman kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Amani,Usalama, Sehemu ya Salama.Neno Aman ndio lililotoa neno Amanatun ambalo humaanisha Amana, Jukumu, Ahadi au Makubaliano.Neno Aman ndio lililotoa neno Iman ambalo humaanisha Imani ambapo tunapozungumzia kuhusiana na Dini ya Kiislam basi neno Imani hua linamaanisha Kua na Ikhlasi na Msimamo katika Dini.

Hivyo Uislam humaanisha Muonekano wa Nje wa Kujisalimisha kwa Allah Subhanah wa Taala na Imam hua ni Muonekano wa Ndani ya Nafsi na Moyo.Na ndio maana ikawa kuna Waislam na kuna Waumini ambapo Waumini hua ni wenye Kuonesha Kuamini kwao kutokana na Vitendo vyenye kutokana na Hisia za Moyoni lakini Waislam huonesha Imani yao kutokana na Muonekano wa Vitendo vyao kwa juu juu.Hivyo kwa Muumini wa kweli basi Imani ya Dini ya Kiislam hua inakipaumbele kisha ndio Hufuatia Uislam wake.

Na wenye Imani Dhaifu basi kwanza hutanguliza Uislam kisha ndio Imani yao.Na hapa ndio utaona tofauti baina yetu Waislam wa Leo na aaliotangulia kwani sisi Waislam wa leo tunajiita WaIslam lakini Imani zetu ni Dhaifu sana.Na huu ndio Mtihani mkubwa zaidi kwa Umma wa Kiislam katika Dunia nzima kwa Ujumla, kwani Alisema Hasa Al Basr kua: '**Hakika mimi nilikutana na Masahaba 70 waliopigana Vita vya Badr, na kama wao wangefufuka leo hii na kukuoneni nyinyi mnvayoishi basi wangesema kua nyinyi hamkuamini, na kama nyinyi mngewaona wao namna walivyokua wakiishi bas mngesema kua wao ni waenda Wazimu.'**

Naam neno Aman ndio lililotoa Jina la kike liitwalo Amina ambalo humaanisha Kua Salama na Kuaminika.Na pia neno Aman ndio lililotoa neno Amiin, ambalo hua ni Kiitikio cha Dua au Maombi au Hitimisho la Surat Al Fatiha.Ambapo neno hili Amiin hua linamaanisha Naamini kua itakua Hivyo au Naam Ikubalie na ndio maana Wanazuoni wakasema kua neno Amiin hua linamaanisha Ya Allah Tukubalie, ambayo hua ni sawa na kusema *Allahuma Istajaba Lana.*

Na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Jibril amenifundisha Mimi Kusema Amiin baada ya Kusoma Surat Al Fatiha na akaniambia kua Amiin kwa Surat Al Fatiha hua ni sawa na Muhuri kwenye Barua.'***(Sunan Abu Daud)*

Naam..amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisoma- *Ghayri Al Maghdhuubi aAlayhim wala Aldhaliin* - Alikua akisema Amiin, ili mtu aliekua Karibu nae katika Safu ya Kwanza aweze kumsikia.***(Imam Abu Daud)*
Na amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Mayahudi hawakuoneeni nyinyi wivu kwa chochote kile kuliko wanavyokuoneeni wivu kwa Salam zenu na Kuitikia kwenu Amiin.'***(Sunan Ibn Majah)*

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Wakati Imam (baada ya kusoma Surat Al Fatiha) atakaposema Amiin basi na nyinyi semeni Amiin**. **Na kama Amiin ya Mtu ikienda sambamba na Amiin ya Malaika basi mtu huyo atasamehewa Dhambi zake zot**e*(Sunan Ibn Majah,Musnad Imam Ahmad, Sunan Abu Daud, Sunan An Nasai, Sahih Bukhari)*

Na amesema Abd Jabbar Ibn Wail kua: '**Ameniambia Baba yangu mimi kua Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisoma G*hayri Al Maghdhuubi aAalayhim wala Al Dhaliin*-basi alikua akisema Amiin na sisi tulikua tukimsikia.'***(Sunan Ibn Majah)***

Ambapo bila ya shaka kila mmoja wetu anajua kua baada ya Kisomo cha Surat Al Fatiha, na baada ya Dua basi hua ni kutikia Amiin.Na hii ni kutokana na kua mbali ya kua kama tulivyosema kua Sala ni Surat Al Fatiha lakini pia tuliona katika Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua *Allah Subhanah wa T'aala*, ameigawa Surat Al Fatiha katika sehemu mbili baina yake na baina ya Mja wake anaeisoma, na akaahidi kua atamlipa Mja wake kile anachokiomba.

Na ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa akiisoma Surat Al Fatiha basi mwisho wake huitikia Amiin, kama zilivyothibiyisha Hadithi ambapo Wanazuoni wanasema kuhusiana na Maana ya neno Amiin hua ni Ya Allah tukubalie maombi yetu.

Ambapo anasema Imam Abu Abd Allah Sahl Ibn Muhammad Al Tustari kua: '**Amesema Muhammad Ibn Sawwar kua amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua:** '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kaeni kwenye Njia iliyonyooka ingawa hamtoweza kufanya mambo mema yote**. **Jueni kua Jambo Jema zaidi kwenu ni Sala, na bila ya shaka ni Muumini wa kweli tu ndie anaetia Udhu kwa Umakini na kikamilifu**. **Na Imam anaposema Amiin baada ya *Ghayri Al Maghdhuubi aAlayhim wala Al Dhaliin* basi Itikieni AmiinKwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni mwenye kumridhia yule anaesema Amiin na anamkubalia Sala yake na kumjibu Dua zake.'**

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi kua: '**Kusema Amiin baada ya Kisomo cha Surat Al Fatiha hua ni Sunnah iwe kwa Mtu anaesoma huku akiwa ndani ya Sala au akia nje ya Sala. Na ni Sunna kusema kwa Amiin kwa Sauti katika Sala za Sauti na kuitikia Amiin kimya kimya kwa Sala za Kimya kimya. Na ni Sunna kwa Imam anaposalisha Kupumzika Kidogo baada ya Ghayri Al Maghdhuubi aAlayhim Wala Dhaliin kabla ya Kusema Amiin. Na hii ni kwa Sababu Neno Amiin si sehemu ya Surat AlFatiha, hivyokupumzika huko huwaonesha Wanaomfuata Imam kua neno Amiin si sehemu ya Surat Al Fatiha.**'*(Al Tibyan)*

Na Wanazuoni wanapendekeza kua kipimo cha Kupimzika huko kabla ya Kusema Amiin kunatakiwa kuwe na ukubwa sawia na wakati utakaomchukua Imam kusema Subhanah Allah kisha ndio asema Amiin

Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi anaendelea kusema kua:

يستحب لكل قارئ كان في الصلاة أو في غيرها إذا فرغ من الفاتحة أن يقول أمين

'Hua ni Wajibu kwa kila Msomaji iwe yumo ndani ya Sala ama nje, kua anapomaliza kusoma Surat Al Fatiha awe anasema Amiin'*(Al Tibyan Fii Adab Hamalah Al Qur'an)*

Na anasema Imam Abu Al Fida Ismail Ibn Umar Ibn Kathir Ad Dimashqi Al Shafii katika Tafsir Ibn Kathir kua:

يُسْتَحَبُّ لِمَنْ قَرَأَ الْفَاتِحَةَ أَنْ يَقُولَ بَعْدَهَا: آمِينَ... قَالَ أَصْحَابُنَا وَغَيْرُهُمْ: وَيُسْتَحَبُّ ذَلِكَ لِمَنْ هُوَ خَارِجُ الصَّلَاةِ، وَيَتَأَكَّدُ فِي حَقِّ الْمُصَلِّي، وَسَوَاءٌ كَانَ مُنْفَرِدًا أَوْ إِمَامًا أَوْ مَأْمُومًا، وَفِي جَمِيعِ الْأَحْوَالِ

Ni Sunnah kwa wale wenye kuisoma Surat Al Fatiha na baada ya Kuimaliza kusema Amiin Na As-hab wetu Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na wengineo zaid yao pia wamesema kua Ni Sunna. **Kwa wale wanaoisoma Surat Al Fatiha Nje ya Sala, ambapo kwa anaeisoma Ndani ya Sala ndio hua Sunna zaidi, iwe mtu huyo anasali peke yake, iwe ni Imam ama iwe ni Maamuma, na katika hali zote***(Tafsir Ibn Kathir)*

Ambapo amesema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

إِذَا قَالَ أَحَدُكُمْ آمِينَ . وَالْمَلاَئِكَةُ فِي السَّمَاءِ آمِينَ . فَوَافَقَتْ إِحْدَاهُمَا الأُخْرَى غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ

Wakati miongoni mwenu anaposema Amin basi na Malaika Mbinguni hua pia wanasema Amiin na Amiin ya yule Mtu itakayoenda Sambamba na ya Malaika basi mtu huyo Husamehewa Dhambi Zake zote zilizotangulia hapo kabla.*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Na kulingana na Hadith hii basi tunaona kua Kuitikia Amiin katika Sala baada ya kisomo cha Surat Al Fatiha ambako hua kunamaanisha kumuomba Allah Subhanah wa Ta'ala atukubalie na pia atusamehe madhambi yetu.Na ndio maana katika *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akafananisha Mwenye Kusali Sala tano na Mtu Mwenye kuishi kwenye Nyumba iliyopo pembeni ya MtoYaani Mtu huyo hatoiwezekana kwake kua Mchafu.

Kwani siku moja*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuona mtu akiomba Dua nzito sana na hivyo akasema:**'Kwa Hakika Atajibiwa Maombi yake na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama ataifunga Dua yake hio.'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: Kwa Kuifunga vipi?

***Rasul Allah Salallahu Alayhi* akajibu: 'Kwa kumalizia Kusema Amiin'** *(Sunan Abu Daud)*

Hivyo kuitikia Amiin hua ni Sunna inayopendekezwa kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Hanifa, Imam Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal na kuna mtizamo mmoja pia juu ya hili kutoka kwa Imam Malik.

Kwani anasema Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki kua: '**Kwa kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* kua: Imam atakaposema Amiin basi na nyinyi semeni Amiin**. **Na kwa kua imethibitishwa kua *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* alikua akiitikia Amiin anapomaliza Kusoma Surat Al Fatiha, basi imekua hakuna mvutano juu ya jambo hili kwani huo ndio Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni, wakiwemo waliosema kua ni mtizamo wa Malik Na waliosema kua ndio Mtizamo wa Watu wa**

Madina na ndio pia Mtizamo wa Hanafi, Shafi, Ahmad Ibn Hanbal na Daud Dhahiri pia'*(At Tahmiid)*

Ambapo amesema Ima Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Amesema Ataa Ibn Abi Rabah kua; Mimi nimezoea Kuwasikia Maimam akiwemo Ibn Az Zubayr na waliotangulia kabla yake, wakiwa ni wenye kusema Amiin na Maamuma walionyuma yao huitikia Amiin hadi kufikia Msikiti Mzima Kujaa Sauti hio'***(Al Umm)*

Na amesema Imam Al Bayhaqi kua: '**Tumenukuu sisi kua kutoka kwa Abd Allah Ibn Umar Radhi Allahu Anhu kua alikua akinyanyua Sauti yake katika wakati wa Kusema Amiin, iwe anapokua Ni Imam au anaposali peke yake.'***(Imam Al Bayhaqi).*

Na Imam Al Bukhari amesema kua: '**Amesema Naafi kua Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kamwe hakua ni mwenye kuachana na kusema Amiin baada ya kusoma Surat Al Fatiha na alikua akituhimiza kufanya hivyo, nami nimesikia mengi mazuri juu ya kufanya hivyo kutoka kwake yeye.'**

Hivyo inapendekezwa Kutikia Amiin baada ya Kisomo cha Surat Al Fatiha na kwa kua kufanya hivyo hua ni Sunna basi ba ya shaka kufanya kwake kaa kuitikia Amiin hua kuna manufaa makubwa zaid kuliko kuiwacha na kutoitikia.Na Hukmu yake pia kaa kua ni Sunna basi kutoifanya kwa kusahau au kwa Makusudi basi hakutoathiri Sala ya Mtu husika na labda kuifanya kua na mapungufu. La, kama vile ambavyo hali inayokua pale tunapoangalia kuhsiana na kusoma Sura ya ziada baada ya Surat Al Fatiha katika Sala.

KISOMO CHA SURA NYENGINE BAADA YA SURAT AL FATIHA

❖❖❖

Amesema Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu* kua:**'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Surat Al Fatiha na Sura nyengine isiyopungua aya 30 katika Rakaa mbili za mwanzoni za Salat Dhuhr na Al Asr na katika Rakaa mbili za mwishoni alikua akisoma Sura yenye aya zisizozidi 15'.** Ambapo huu pia ni mtizamo wa Imam Al Shafii Mwenyewe.

Hivyo hapa tunakumbushana tena kua **Kusoma Sura Al Fatiha katika Kila Rakaa hua ni Wajib kwani Surat Al Fatiha ndio Sala yenyewe na hivyo Ndio Nguzo kuu ya Sala**: **Na kusoma Sura nyengine yeyote Baada ya Surat Al Fatiha hua ni Sunna, nakuna mitizamo miwili kama tulivyoiona katika Hadith mbili tulizoanza nazo.**

Na kwa kua ni Sunna kusoma Sura nyengine baada ya Surat Al Fatiha Basi inapendekezwa Katika Rakaa ya Tatu na ya Nne kusoma Surat Al Fatiha tu.

Kwani anasema Imam An Nawawi kuhusiana na Hadith ya Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Hadith hii inaonesha kua Kusoma Sura fupi baada ya Surat Al Fatiha hua ni bora kuliko Sehemu ya kipande cha Sura ndefu.'***(Sharh Sahih Muslim)*

Na Imam Ibn Hajar Al Asqallani amesem kua:**'Maneno yasemayo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma yanaoesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua ni mwenye kudumu Katika kufanya Hivyo katika Sala***(Fat-h Al Barr)*

Na hivyo basi kulingana na Hadith hizi basi hua inapendekezwa kusoma Sura Ndefu zaidi katika Rakaa ya kwanza na kisha Sura Fupi yake au Sura zenye urefu sawia wa Aya katika rakaa ya pili baada ya Surat Al Fatiha. Na haipendekezwi kusoma Sura fupi kwenye Rakaa ya kwanza na kisha Sura ndefu kwenye Rakaa ya pili. Yaani kwa mfano kwanza ukaanza na Surat Al Kawthar na kisha ukamalizia na Sura Al Aalaq.

Na unaweza kusoma Aya Moja ndefu kama Aya Nur, Ayat Al Qursiyyu n.k baada ya Sura Al Fatiha au ukasoma Aya fupi zisizopingua Tatu kama za Surat Al Kawthar. Ambapo amesema Ikrimah na Al Aswad kua:Kuna mtu alikuja kwa Ibn Masud na kusema kua: **'Jana mimi nilisoma Mufassal katika Rakaa moja.'**

Mufassal ni sehemu ya Sura fupi za Qur'an kuanzia Surat Qaf hadi Surat An Nas.

Hivyo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: '**Hio ni rahisi sana ni sawa na kusoma Mashairi**. **Mimi nnazijua Sura mbilimbili ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akizisoma katika Rakaa moja.Alikua akisoma Surat Ar Rahman na Surat An Najm katika Rakaa moja, alikua akisoma Surat Al Qamar na Surat Al Haqqah katika Rakaa moja, au Surat Tur na Dharriyat katika Rakaa moja au Surat Al Waqiah na Al Qalam katika Rakaa moja, Surat Marij na Surat Naziat, katika Rakaa moja, Surat Al Mutaffifn na Abbasa katika Rakaa moja, Surat Al Muddathir na Muzzamil katika Rakaa moja, Surat Al Insan na Al Qiyamah katika Rakaa moja, Surat An Nabaa na Mursalat katika Rakaa moja, Ad Dukhan na At Takwir katika Rakaa moja***(Imam Abu Daud)*

Na hadith hii inatuonesha kua inaruhusiki kusoma Sura zaidi ya Moja baada ya Surat Al Fatiha katika Sala.

Neno Mufassalat hua linamaanisha kitu ambacho kimeambatana kimsururu katika kufutana na hivyo katika Qur'an kuna Sura ndogo ndogo ambazo zimefuatana na kutengenishwa baina yao na *Bismi Allahi Rahmani Rahiim.*Ambapo anasema *Ummu Ul Muuminina* Aisha *Radhi Allahu Anha* katika hadith ya Ibrahim Ibn Musa isemayo kuhusiana na Surat Al Mufassalat kua:

حَدَّثَنَا إِبْرَاهِيمُ بْنُ مُوسَى، أَخْبَرَنَا هِشَامُ بْنُ يُوسُفَ، أَنَّ ابْنَ جُرَيْجٍ، أَخْبَرَهُمْ قَالَ وَأَخْبَرَنِي يُوسُفُ بْنُ مَاهَكَ، قَالَ إِنِّي عِنْدَ عَائِشَةَ أُمِّ الْمُؤْمِنِينَ ـ رضى الله عنها ـ إِذْ جَاءَهَا عِرَاقِيٌّ فَقَالَ أَىُّ الْكَفَنِ خَيْرٌ قَالَتْ وَيْحَكَ وَمَا يَضُرُّكَ قَالَ يَا أُمَّ الْمُؤْمِنِينَ أَرِينِي مُصْحَفَكِ. قَالَتْ لِمَ قَالَ لَعَلِّي أُوَلِّفُ الْقُرْآنَ عَلَيْهِ فَإِنَّهُ يُقْرَأُ غَيْرَ مُؤَلَّفٍ. قَالَتْ وَمَا يَضُرُّكَ أَيَّهُ قَرَأْتَ قَبْلُ، إِنَّمَا نَزَلَ أَوَّلَ مَا نَزَلَ مِنْهُ سُورَةٌ مِنَ الْمُفَصَّلِ فِيهَا ذِكْرُ الْجَنَّةِ وَالنَّارِ حَتَّى إِذَا ثَابَ النَّاسُ إِلَى الإِسْلاَمِ نَزَلَ الْحَلاَلُ وَالْحَرَامُ، وَلَوْ نَزَلَ أَوَّلَ شَىْءٍ لاَ تَشْرَبُوا الْخَمْرَ. لَقَالُوا لاَ نَدَعُ الْخَمْرَ أَبَدًا. وَلَوْ نَزَلَ. لاَ تَزْنُوا. لَقَالُوا لاَ نَدَعُ الزِّنَا أَبَدًا. لَقَدْ نَزَلَ بِمَكَّةَ عَلَى مُحَمَّدٍ ﷺ وَإِنِّي لَجَارِيَةٌ أَلْعَبُ {بَلِ السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَدْهَى وَأَمَرُّ} وَمَا نَزَلَتْ سُورَةُ الْبَقَرَةِ وَالنِّسَاءِ إِلاَّ وَأَنَا عِنْدَهُ. قَالَ فَأَخْرَجَتْ لَهُ الْمُصْحَفَ فَأَمْلَتْ عَلَيْهِ آىَ السُّوَرِ.

Amesema Hisham Ibn Yusuf, kua amesema Anaa Ibna Jurayj kua amesema kua ametuambia sisi Yusuf Ibn Mahaka kua: **'Wakati nilipokua na Aisha *Ummu Ul Muuminina Radhi Allahu Anha,* alikuja mtu kutoka Iraq na akamuuliza: ' Ewe*Ummu Ul Muuminina* Hivi jee ni Sanda gani ndio bora zaidi?'**

Aisha *Ummu Ul Muuminin Radhi Allahu Anha, akasema: 'Allah akuingize kwenye Reahma zake, itakusaidia nini jibu lake?*' Muiraq huyo akasema: 'Ewe *Ummu Ul Muuminin* hebu nioneshe Msahafu wako.'Aisha *Ummu Ul Muuminin Radhi Allahu Anha* akauliza: 'Ya nini?'

Muiraq akajibu: 'Kwa ajili ya kuikusanya na kuipanga Qur'an katika mpangilio wake. Kwani kuna watu wanaisoma bila ya mpangilio wake.'

Aisha *Ummu Ul Muuminin Radhi Allahu Anha* akasema: 'Jee kuna umuhimu gani wa sehemu gani yake kuisoma kabla (ama la bali unatakiwa ujue kua) Sehemu ya mwanzo kushushwa kutokana nayo, ni Sura miongoni mwa Surat Mufassalat ambazo ndani yake mmezungumziwa kuhusiana na Pepo na Moto, na watu walipoukumbatia Uislam, zikashushwa aya zilizozungumziwa yaliyohalalishwa na yaliyoharamishwa, kwani kama jambo la kwanza kushushwa lingekua: 'La Tashrabu Al Khamr – Msinywe Ulevi' basi watu wangkua ni wenye kusema kua, Kamwe hatutoacha Ulevi.' Na kama ingeshushwa: 'La Tazanu - Msizini'. Basi watu wangelikua ni wenye kusema: 'Kamwe hatutoacha Zina'

Wakati mimi nilipokua mdogo katika umri wa kucheza, basi ilishushwa aya ifuatayo katika Mji wa Makkah kwa Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam:*

﴿بَلِ ٱلسَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَٱلسَّاعَةُ أَدْهَىٰ وَأَمَرُّ﴾

Bali alss<u>a</u>AAatu mawAAiduhum waalss<u>a</u>AAatu adh<u>a</u> waamarru*(Surat Al Qamar 54:46)*

*Tafsir:**Bali Saa ndio wakati walioahidiwa (kwa ajili ya Malipo yao) na Saa itakua ni yenye Maumivu Makubwa sana.***

Kasha Surat Al Baqara na Surat An Nisaa ikashushwa wakati nikiwa pamojanae. Na kisha Aisha Ummu ul Muuminina *Radhi Allahu Anha*akachukua Msahafu wake na akamnukulia aya za Qur'an za Sura na mpangilio wake.

Na Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Surat Mufassalat kwani kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: **'Kuna Mufassalat ndefu ambazo zimeanzia na Surat Al Hujurrat na kumalizikia katika Surat Al Buruj, na baada ya hapo kuna Mufasalat za urefu wa kati ambazo zimemalizikia kwenye Surat Al Bayyina na kisha kuna Mufassalat fupi ambazo zinaanzia baada ya hapo hadi mwisho katika Surat An Nas.'**

Ama upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: **'Kuna Mufassalat ndefu ambazo zimeanzia na Surat Al Hujurrat na kumalizikia katika Surat An Naziat na baada ya hapo kuna Mufasalat za urefu wa kati ambazo zimeanzia na Surat Abbasa na zimemalizikia kwenye Surat AlDhuha na kisha kuna Mufassalat Fupi ambazo zinaanzia baada ya hapo hadi mwisho katika Surat An Nas.'**

Ama upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua: **'Kuna Mufassalat ndefu ambazo zimeanzia na Surat Al Hujurrat na kumalizikia katika Surat Al Qamar na Ar Rahman**

na baada ya hapo kuna Mufasalat za urefu wa kati ambazo ni kama Surat Shams na Surat Al Layl na Mufassalat kama Surat Al Asr, Al Ikhla,Surat An Nas.nk'

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: **'Mufassalat zimeanzia kwenye Surat Qaf na hii ni kwa sababu ya hadith ya Aws Ibn Hudhayfah *Radhi Allahu Anhu* ambae anasema kua: Mimi niliwauliza Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kuhusina na namna walivyoigawa Qur'an ambapo nao waliniambia kua: 'Ni katika Hizbu Tatu na Tano, na Saba na Tisa, na Kumi na Moja na Kumi na Tatu.'*** ***(Imam Abu Daud, Imam Ibn Majah)***

Hivyo Hizb ya kwanza ina Sura tatu, Hizb ya pili ina Sura Tano zinazofuatia baada yake, Hizb ya Tatu ina Sura Saba zinazofuatia baada yake, Hizb ya Nne ina Sura Tisa zinazofuatia baada yake, Hizb ya Tano ina Sura Kumi na Moja zinazofuatia baada yake, Hizb ya Sita ina Sura Kumi na Tatu zinazofuatia baada yake kwa mpangilio huo na hivyo Hizb Mufassala hua ni Hizbu ya Sura za Mwisho za Quran ambazo zimeanzia kwenye Sura ya 49 ya Qur'an kwa kuhesabu kutoka kwenye Surat Al Baqara.

Na amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimchagua Mtu kua Imam katika kikundi cha Jeshi,na Mtu huyo akawa kila siku akisalisha basi katika Kisomo chake lazima amalizie na Surat Al Ikhlas**. **Baada ya jeshi hilo kurudi Madina, Wanajeshi wakamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* namna alivyokua akisoma Imam wao huyo.'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hebu Muulizeni kwanini alikua akifanya hivyo?'**

Baada ya kuulizwa basi Mtu huyo akajibu: 'Kwa Sababu Sura hii ina Sifa Tukufu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hua naipenda kuisoma.*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoambiwa hivyo basi akasema: Mwambieni kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anampenda nae pia.*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo kwa upande wa Ubaidah Ibn Samit *Radhi Allahu Anhu* anasema kua**: 'Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:Mmoja katia ya Maansari alikua ni Imam wa Masjid QubahNa alikua akisalisha basi (baada ya Surat Al Fatiha) alikua lazima asome Surat Ikhlas na kisha husoma Sura nyengine, katika Kila Sala**. **Hivyo watu wakamwambia: Kila siku wewe hua unaanza na Surat Ikhlas Lakini sisi tunaona kua haikutoshelezi hadi usome na Sura nyengine juu yake kwanini?'**

Mtu huyo akajibu kwa kusema: 'Siwezi kuacha kufanya hivyo, kwani napenda kukuongozeni katika Sala kwa kufanya hivyo, hivyo kama nyinyi hamtaki basi mimi nitaachana nanyi na sitosalisha.'

Watu hao wakatafakari na kumuona Imam wao ni mbora miongoni mwao, hivyo haina haja kusalishwa na Imam mwengine. **Na hivyo wakamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae akamwambiaMtu huyo: Ewe Fulani Ibn Fulani hivi ni kitu gani kilichokuzuia wewe usifanye kila walichokuambia watu wako? Kwanini unasoma Surat Ikhlas katika kila Rakaa?'**

Mtu huyo akajibu: 'Hakika mimi Naipenda Sana Sura hio.'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kumwambia Mtu huyo kua: Kuipenda kwako Sura hio kutakupelekea kuingia Peponi(Fiqh Sunnah)*

Na vile vile anasema Imam Abu Daud kua: **Kuna Mtu kutoka katika Ukoo wa Juhaynahambae amesema kua: 'Nimemsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisoma Idha Zulzilat Al Ardhu Zilzalaha, katika Rakaa zote mbili wakati alipokua akitusalisha sisi Sala ya Alfajir**. **Lakini sikuweza kujua kama alisahau kua ameshaisoma au aliirudia kuisoma kwa Makusudi'***(Imam Abu Daud)*

Kwani Hadithi mbili za kwanza ni Hadith zinazotuonesha kua kuna mambo ndani ya Ibada ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakua akiyafanya Yeye Ila Masahaba walikua wakiyafanya na hayakua ni Bidaa, kwa sababu tu hayakufanywa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Hivyo ingawa mambo hayo hakuyafanya yeye lakini kwa kua ni mazuri basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliyaridhia kutokana na Uzuri wake, Tofauti na wanavyoona wengi leo hii kua Jambo ambalo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakulifanya hata kama ni jema basi ni Bidaa na ni Haram.

Jambo la pili tunaloliona katika Hadith zote hizi tatu kwa ujumla kuhusiana na Kisomo katika Sala baada ya kusoma Surat Al Fatiha basi ni kua Inaruhusika kuirudia tena Sura hio hio moja baada ya Surat Al Fatiha, iwe kwa sababu ya kua Mtu anaesali hana Sura nyengine anayoijua baada ya Surat Al Fatiha na Sura hio husika tu, au labda iwe ni kutokana na kuipenda zaidi Sura Husika n.k.

Kwani pia amesema Shaykh Ul Islami Imam Zakarriya Al Ansari kua: **'Zayd Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alisoma Surat Al Araf katika Rakaa zote mbili za Salat Al Maghrib'na amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiigawa Surat Al Baqara katika Rakaa mbili.'**

Na Imam Al Zuhri amesema kua: 'Anas ameniambia mimi kua: **'Abu Bakr alitusalisha Sala ya Alfajir na hivyo akaanza na Surat Al Baqara na akasalisha kwa kuisoma katika Rakaa mbili kutokana nayo, na alipomaliza na kutoa Salam basi Umar Ibn Al Khattab akamwambia Abu Bakr kua: 'Tumemaliza kusali bado kidogo tu Jua lichomoze' Abu Bakr akasema: 'Kama lingechomoza basi lingetufuata bila ya kua nadharau.'''**

Na *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* alisali na akasoma *Surat Al Muuminun* na alipofikia katika aya inayomtaja Isa Ibn Maryam isemayo:

﴿وَجَعَلْنَا ٱبْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُۥٓ ءَايَةً وَءَاوَيْنَٰهُمَآ إِلَىٰ رَبْوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَمَعِينٍ﴾

WajaAAalna ibna maryama waommahu ayatan waawaynahuma ila rabwatin dhati qararin wamaAAeenin*(Surat Al Muuminun 23:50)*

*Tafsir**: Na tukamjaalia Ibn Maryam na Mama yake kua kama ni dalili na tukawapa hifadhi katia sehemu ya juu ya Ardhi, sehemu ya kupumzikia na usalama na chemche zenye kutiririka.***

Basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaanzakulia na kisha akarukuu.'

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hnbal kua amesema Ibn Abzi kua: **'Nilisali mimi nyuma ya Umar Ibn Al Khattab na akasoma Surat Yusuf na alipofika ile aya isemayo'**

﴿وَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَٰٓأَسَفَىٰ عَلَىٰ يُوسُفَ وَٱبْيَضَّتْ عَيْنَاهُ مِنَ ٱلْحُزْنِ فَهُوَ كَظِيمٌ﴾

Watawall<u>a</u> AAanhum waq<u>a</u>la y<u>a</u> asaf<u>a</u> AAal<u>a</u> yoosufa waibyad<u>d</u>at AAayn<u>a</u>hu mina al<u>h</u>uzni fahuwa ka*<u>dh</u>*eemun *(Surat Yusuf 12:84)*

Tafsiri: ***Akageukia (Nabii Yaqub) upande mwengine na akasema Ah! Huzuni yangu kubwa iko kwa Yusuf! na yakawa Meupe Macho Yake (Nabii Yaqub) Kutokana na Huzuni aliyokua ameigubika (Moyoni)***

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akaanza kulia, hivyo akainama na kisha akanyanyuka na kusoma Surat An Najm na akasjudu kutokana nayo na alipokuja juu akasoma Idha Zulzilat.

Mfano mwengine ni ule wa Sahaba aitwae Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu.*Ambae alikua pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Jeshi lake wakielekea katika maeneo ya Najd.Usiku ukawafikia wakati wakiwa njiani, hivyo wakapiga kambi. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: '**Jee ni nani na nani leo hii watakua walinzi wa Usiku'**

Ambapo Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* na Ammar Ibn Yassir *Radhi Allahu Anhu*waliokua ndugu wa Kiimani waliounganishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya Ammar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* kuhamia katika mji wa Madina walikua ni marafiki wakubwa sana kwani katika kila sehemu na kila kitu walikua wakipenda kua pamoja, hivyo katika Usiku huo wakasema kua wao watakesha kulinda.

Hivyo kwa kua Usiku huo ulikua shwari sana, hivyo Abbad Ibm Bishr *Radhi Allahu Anhu*akamwambia Ammar Ibn Yasir*Radhi Allahu Anhu* kua:'**Hamna tatizo Wewe lala kisha baadae nitakuamsha, kisha nitalala mie wewe utalinda**.' Hivyo Ammar *Radhi Allahu Anhu*akalala.

Hivyo Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu*akaona kua Usiku huo uliokua shwari ni Mzuri sana kwa ajili ya Kufanya Ibada kwa kusali Qiyam Al Layl, hivyo akatia Udhu na kuanza Kusali kwani Ammar Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu*alikua akijulikana kama Rafiki wa Qur'an. Kwa sababu alikua anapenda sana kusoma na akitiririka basi anatiririka kweli utapenda umsikilize tu anavyotiririka na aya za Qur'an. Hivyo akaanza Kusali na kuanza Kutiririka.

Hivyo Wakati anatiririka na Qiraa cha aya 110 za Surat Al Kahf ndani ya Sala mara ghafla akashtukia Upinde wa Mshale umepika kwenye Bega lake.Lakinihata hivyo Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu*hakukatisha Qiraa wala Sala yake, bali alinyanyua mkono wake akaukata Upinde huo na kisha akaendelea kutiririka na Qiraa chake hadi akamaliza, akarukuu akasjudu akaja juu tena kwenye kutiririka katika Kiraa cha rakaa ya pili.

Ghafla Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu*akapigwa Upinde wa pili.Subhana Allah! Abbad Ibn Bishr*Radhi Allahu Anhu* kamwe hakukatisha Kutiririka na qiraa chake bali aliukata Upinde huo na akaendelea na Sala mpaka akamaliza, huku akiwa ataabani hana nguvuhivyo akamwamsha Ammar Ibn Yassir *Radhi Allahu Anhu* na kumwambia: **'Aamka kwani mimi nimejeruhiwa'**

Ammar *Radhi Allahu Anhu*akamuuliza: **"Kwanini hukuniamsha pale ulipopigwa upinde wa kwanza?"**

Abbad *Radhi Allahu Anhu*akasema: **'Kwa sababu nilikua katikati ya kisomo cha Aya za Qur'an ambazo zilikua zimenifunika ndaniya Moyo wangu kwa Utamu wake na hivyo sikutaka kukikatisha kisomo hiki kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliniamrisha mimi kuihifadhi Moyoni Sura hii, hivyo kwangu mimi kifo ni bora kuliko kukatisha kisomo cha Sura h hii.'**

Naam..huyo ndio Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* na Khushuu katika Sala yake, ambae hata hivyo hakufa katika wakati huu bali alifariki katika Vita vya Yamamah alipopigana huku akiwa chini ya Uongozi wa Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu.*

Hivyo tumemalizana kuhusiana na Nguzo ya nne ya Sala ambayo ni Qiraat Surat Al Fatiha pamoja na Suna zake nahivyo tunaingia katika Nguzo ya tano ya Sala ambayo ni Rukuu.

5-RUKUU

❖❖❖❖

﴿وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَاةَ وَآتُواْ ٱلزَّكَاةَ وَٱرۡكَعُواْ مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

Waaqeemoo alssalata waatoo alzzakata wairkaAAoo maAAa alrrakiAAeena*(Surat Al baqara 2:43)*

Tafsir: ***Na Simamisha Sala, Na Utoe Zakkah, Na Jisalimishe na Kujinyenyekesha kwa Kurukuu Pamoja na Wenye Kurukuu.***

Neno Raka'a kwa Lugha Ya Kiarabu hua linamaanisha Kuinama, Kupinda mgongo kuelekea Chini kwa mbele, Kua na Mgongo Uliopinda, Kurukuu katika Sala, Kugusisha Kichwa Kwenye Magoti, Kusali na pia humaanisha Kitendo cha Mtu mwenye Kumuabudu Allah Subhanah wa Ta'ala anachokifanya baada ya kusimama na kisha akainama na kuiweka Mikono yake Magotini bila ya kupinda Mikono wala Miguu yake.

Neno Raka'a ndio kililotoa neno Rakiuun yaani Watu wenye Kurukuu katika Ibada ya Sala ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ambavyo ndivyo alivyoaamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kwa kusema:

﴿وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَاةَ وَآتُواْ ٱلزَّكَاةَ وَٱرۡكَعُواْ مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

Waaqeemoo alssalata waatoo alzzakata wairkaAAoo maAAa alrrakiAAeena***(Surat Al Baqara 2:43)***

Tafsir: Na Simamisha Sala, Na Utoe Zakkah, Na Jisalimishe na Kujinyenyekesha kwa KurukuuPamoja na Wenye Kurukuu.

Aya imetaja neno Sala na kisha pia Ikataja Zakkah na ikataja Sehemu ya Kitendo cha Ndani ya Sala ambacho ni Kurukuu.

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametaja hali hizi mbili tofauti ambazo kwa baadhi hua zinaweza kua ni Moja, lakini ukweli ni Kua tunapozungumzia Sala basi hua ni Mjumuiko wa Vitendo na Kauli za Ibada ya kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama tulivyofikishiwa na *Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kupitia kwa Malaika Jibril Alayhi Salam.

Na tunapozungumzia Kurukuu basi hua tunazungumzia hali ya Unyenyekevu inayotakiwa mtu kua nayo wakati anapokua katika Ibada ya Sala

Ambapo bila ya shaka Unyenyekevu hua ni wenye kutokana ndani ya Moyo wa Mtu kulingana na Imani yake na ndio maana tukasema kua Kuna Waislam na Waumini.

Yaani Muumini hua na Imani Thabit na hua ni Mwenye Kurukuu ipasavyo kwa unyenyekevu. Na Muislam hua na Imani ya Kawaida au Dhaifu kabisa na hivyo Rukuu yake hua haina Unyenyekevu.

Hivyo ingawa wote hawa ni Waislam na Wanasali lakini Waumini ndio hua na sifa ya Maa Al RakiiAaina - Wenye Kurukuu ipasavyo kwa Unyenyekevu ndani ya Sala zao.

Na ndio maana pia Rukuu ikawa ni Nguzo ya Sala, kwani ndio iliyotoa neno Rakaa yaani Mjumuiko wa Hatua ya Kufunga Sala,Kusoma Surat Al Fatiha, Kurukuu, Kusimama, Kusjudu na Kusimama au Kukaa Tahiyyat.

Kwani Aya hii pia imejumuisha ndani yake Mambo matatu ambayo ni Sala, Zakkah na Rukuu kwa Sababu:

Sala Humfanya Mja Kupunguza Matamanio ya Kupenda Madaraka

Zakkah Humfanya Mja kupunguza Matamanio ya Kupenda Mali

Rukuu ya Kweli humfanya Mja Kua Mnyenyekevu na kumuondolea Hisia za Kibr, Wivu na Kujiona

Àmbapo haya ndio Maradhi ya aina tatu Kupenda Madaraka, Kupenda Mali na Kijiona ndio Maradhi waliyokua nayo watu Israil na bado Wanayo pia kama tunavyoona kwa vithibitisho vilivyowazi leo hii katika wakati wa huu wa Uhai wetu kwa mauaji wanayoyafanya nchini Falestina.

Amesema Abu Masud Al Badr *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **hua haihesabu Sala ya Mtu ambae hakunyoosha Mgongo katika wakati wa Kurukuu na Kusjudu.’***(Imam Ibn Hibban, Imam Ibn Khuzaimah na Imam At Tabarani)*

Na akasema Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Mwizi Mbaya zaidi ni yule anaeiiba kutoka ndani ya Sala yake.**

Masahaba Radhi Allahu Anhum **wakauliza: Ya Rasul Allah! Hivi itakuaje hadi Mtu awe ni mwenye kuiba kutoka ndani ya Sala yake?.’**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akajibu: Kwa kutotimiza Rukuu zake na Sijda zake kwa Ukamilifu***(Imam Al Hakim, Imam Ahmad)*

Naam, tuko katika kuangalia kuhusiana na Nguzo ya Tano ya Sala ambayo ni Rukuu, na kama zinavyoonesha Hadith basi tunaona kua kutokana na kua ndio yenye kuonesha unyenyekevu basi Rukuu hua inatakiwa kua ni yenye kutekelezwa kiukamilifu.

Na tunapozungumzia kuhusiana na Ukamilifu basi hua tunamaanisha kua Mtu anapoinama na kurukuu katika Sala baada ya kumaliza Kusoma Kisomo cha Qur'an katika Kisimamo basi Anyanyue mikono

hadi usawa wa mabega au zaidi na hukua akisema Allahu Akbar na kisha awe ni mwenye kurukuu huku akihakikisha kua katika kurukuu kwake kua Mgongo wake uwe Umenyooka Sawia Kuelekea Kibla.

Yaani Miguu yake iwe imesimama sawia haikupinda kwenye magoti huku Mgongo wake ukiwa Umelala na kunyooka katika Usawa wa moja kwa moja kiasi ya kua Kama akimwagiwa Maji mgongoni basi Maji hayo hayatokimbilia Kichwani wala Kiunoni bali yatabakia hapo hapo mgongoni kwenye Uti wa Mgongo.

Hivyo mgongo unatakiwa kunyooka katika Usawa wa moja kwa moja huku akiwa amejizuia kwa Mikono ambayo visugudi vyake vimejitenga na sehemu za Tumbo lake Mwili wake na vidole vya mikono yake viwe vimetanuka na kuyashika Magoti yake huku Shingo na kichwa chake vikiwa vimekaa sambamba ya usawa wa mgongo na mtu husika akiwa amejawa na Utulivu ndani yake.

Ambapo kunyoosha Mgongo huko hua ni Sunna ambayo ni yenye Malipp makubwa zaidi.Ingawa Kutonyoosha Mgongo hukuifanyi Sala husika kua Batili kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Hanifa lakini kufanya hivyo huitia Sala Kasoro inayokupunguzia Malipo ya Sala yako kwa sababu unapokua hukunyoosha Mgongo basi unakua umekosa Unyenyekevu stahiki.Na kila hatua ya ndani ya Sala hua ina malipo yake kulingana na namna Unavyoitekeleza kwa Utulivu na Unyenyekevu.

Kwani amesema Musab Ibn Saad kua: '**Mimi nisali pamoja na Baba yangu, na nikaweka viganja vyangu kwenye Mapaja yangu (Katika Kurukuu) na Baba yangu akanitakza na kusema:Sisi tulikua tukifanya hivyo hivyo lakini tukakatazaa kufanya hivyo na tukaambiwa kua tuweke Viganja vyetu kwenye magoti yetu.'***(Sahih Bukhari)*

Na Imam An Nasai anasema kua:

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ، قَالَ حَدَّثَنِي أَبُو دَاوُدَ، قَالَ حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، عَنِ الأَعْمَشِ، عَنْ إِبْرَاهِيمَ، عَنْ أَبِي عَبْدِ الرَّحْمَنِ، عَنْ عُمَرَ، قَالَ سُنَّتْ لَكُمُ الرُّكَبُ فَأَمْسِكُوا بِالرُّكَبِ .

Muhammad Ibn Bashar amesema kua Abu Dawud kua amesema Shu'bah kua amesema Al A'mash, kua amesema Ibrahim, kua amesema Abu Abdul Rahman, kua amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: "Magoti yametengenezwa kwa ajili yako, basi shikilia magoti.".(Imam An Nasasi)

أَخْبَرَنَا سُوَيْدُ بْنُ نَصْرٍ، قَالَ أَنْبَأَنَا عَبْدُ اللَّهِ، عَنْ سُفْيَانَ، عَنْ أَبِي حَصِينٍ، عَنْ أَبِي عَبْدِ الرَّحْمَنِ السُّلَمِيِّ، قَالَ قَالَ عُمَرُ إِنَّمَا السُّنَّةُ الأَخْذُ بِالرُّكَبِ .

Anasema Suwayd Ibn Nasr kua amesema Abdullah kua amesema Sufyan, kua amesema Abu Husayn, kua amesema Abu Abdul Rahman Al Sulami, akua amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua:'Kwa hakika Ni Sunnah kukamataMagoti'. (Imam An Nasasi)

Na akasema Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliporukuu aliweka mikono yake kwenye Magoti yake kama kwamba ameyakamata huku mikono yake ikiwa imenyooka na kua mbali na Mbavu zake.'***(Sunan Abu Daud)*

Na akasema Imam At Tabarani kua:**'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alipokua akirukuu alikua akiunyoosha Mgongo wake na kuuweka sawa kiasi ya kua akimwagiwa maji basi hayatoondoka Mgongoni mwake.'**

Hivyo kabla hatujazama zaidi katika yanayotakiwa kufanyika Ndani ya Rukuu basi kama ilivyokua kwa Upande wa Qiyam kua tuliangalia kwa upande wa Mwanamme na Mwanammke basi na Katika Rukuu pia inabidi tufahamishane kwa sababu miongoni mwa Wasomaji ni Wanawake na miongoni mwa Wanaume pia wana Mabinti ambao kwa baadhi hua inabidi wawafundishe Kusali.

Na hivyo isije ikawa na Binti kwa sababu anafundishwa na Baba basi nae akasali kama Mwanamme.

Na amesema Imam Al Bayhaqi kua:**'Sharia zote za Sala zinazotofautisha baina ya Sala ya Mwanamme na Mwanammke hua zinasimamia kwenye Satr(Kujisitiri)'**

Hivyo kwa kua kwa upande wa Mwanamke kinachotiliwa mkazo zaid hu ni Kujistiri kwake na kutojitanua na kujikuzisha katika Sala kutokana na Maumbile yake, na hivyo hata katika kufunga mikono anatakiwa afunge kifuani basi hata Rukuu yake hua ni tofauti na ya Mwanamme.

Hivyo wakati kwa Upande wa Mwanamme Mikono yake inatakiwa isigusane na Mwili wake na vidole avitanue kama anashika magoti. Lakini kwa Mwanammke basi yeye hua ni kinyume chake kwani Mikono yake inatakiwa iwe karibu na mwili wake halafu vidole havitakiwi kukamata Magoti kama mwanamme bali vinatakiwa viguse tu magoti yake na anatakiwa asivitanue.

Na kwa maana hio basi Mgongo wa Mwanammke katika Rukuu hautakiwi Kunyooka Sawia kwani kutokana na Maumbile yake. Akifanya hivyo itakua kama amejibinua na tayari anaonesha Uzuri wa Maumbile yake ambayo hatakiwi kuyaonesha na hivyo anapokua katika hali kama hio basi hua hawezi kua na Unyenyekevu ndani yake.

Hivyo Rukuu ya Mwanammke inatakiwa imuoneshe kua amerukuu kwa kuinama kidogo tu kiasi ya kua Vidole vya mikono yake vilivyoshikana vimegusa tu magoti ambayo yamekaribiana na Kichwa kikiwa kinaangalia Chini.

Kwani amesema Imam An Nawawi kua:

قال الشافعي في المختصر ولا فرق بين الرجال و النساء في عمل الصلاة إلا أن المرأة يستحب لها أن تضم بعضها إلى بعض وأن تلصق بطنها بفخذيها في السجود كأستر ما تكون وأحب ذلك لها في الركوع وفي جميع الصلاة

'Amesema Imam Al Shafii katika Al Mukhtasar kua, hakuna tofauti baina ya Sala ya Mwanamme na Mwanamke isipokua Mwanamke anatakiwa aubane na kuukusanya pamoja Mwili wake na Tumbo lake ligusane na Mapaja yake katika Kusjudu, kwani hivyo hua ni Kujihifadhi kunakopendekezwa zaidi katika Rukuu na katika hatua nyengine za Sala pia'*(Al Majmuu)*

Na anasemaSayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafi kua:**'Mwanamke anatakiwa ainame kidogo tu katika Rukuu, hatakiwi**

kutanua vidole vya mikono bali aviweke pamoja, agusishe mikono yake kwenye Magoti na ajitahidi kujikusanya zaidi katika Rukuu na Sujud'*(Radd Al Mukhtar)*

'Ambapo amesema Imam Ibn Jurayj kua: '**Mwanamke hua anajikusanya anaporukuu na anaponyanyua mikono yake basi huinyanyua hadi kwenye usawa wa Tumboni mwake, na kujikusanya pamoja kwa kadri atakavyoweza, atakapo sujudu anaweka mikono yake. Karibu ya mwili wake na Tumbo lake na Kifua chake anaweka karibu na Mapaja yake na kujikumbatia kwa kadri atakavyoweza, kwani Mwanammke ana Maumbile ya Muonekano wa Mikao (Katika Kuinama, Kusujudu na Kukaa) ambayo Mwanamme hua hana, hivyo Mwanamke kama akiachana nayo Mikao hio (Katika Sala) basi hua hana kosa***(Musanaf Ibn Abi Shayba)*

Na wanasema Imam Hasan Al Basr na Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kua:

أن تضع ذراعها وبطنها على فخذيها إذا سجدت، ولا تتجافى كما يتجافى الرجل، ولكي لا ترفع عجيزته

'**Mwanamke (Anaporukuu na) anaposjudu hua anajikunyata kwa kadri awezavyo na hanyanyui sehemu ya Nyuma ya Kiuno chake Juu'**(*Musanaf Ibn Abd Razzak)*

ADHKARI ZA RUKUU

❖❖❖

Ama kuhusiana na Dhkr Allah inayotamkwa katika wakati wa Rukuu basi Mujtahid Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Al Mundhir Al Nishapuri Al Shafii kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala*** **aliposhusha Aya isemayo:**

﴿فَسَبِّحْ بِٱسْمِ رَبِّكَ ٱلْعَظِيمِ﴾

Fasabbi<u>h</u> biismi rabbika alAAa*<u>dh</u>*iimi*(*Surat Al waqiah 56:74,56:96)*

Tafsir: ***Hivyo Litukuza kwa Utukufu wake Jina la Mola wako Mtukufu***

Basi*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*aliwaambia Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kua: 'Semeni Maneno Haya *Subhanah Rabbi Al Aadhiim* ndani ya Rukuu zenu.''

Na hii ni kulingana na Hadith ya Uqbah Ibn Amr *Radhi Allah Anhu* isemyo:

عن عُقبةَ بنِ عامرٍ رضيَ اللهُ عنه، قال: ((لَمَّا نزلَتْ: فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ، قال رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم: اجعَلوها في رُكوعِكم، فلمَّا نزلَتْ: سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى، قال: اجعَلوها في سجودِكم))

Amesema Uqba Ibn Amr *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Iliposhushwa *Fasabih BihamdI Rabbika Al Adhiim*, basi alisema *Rasul Allah Salallahuu Aalayhi wa Salam* kua: 'Ijaalieni hii kua katika

Rukuu zenu, na iliposhuka *Sabihisima Rabbika Al Aala basi Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alisema kua: 'Ijaalieni hii katika Sujudu zenu'''

Ambapo hadith hii ni yenye kuoenesha Asili ya Dhikr hii tunayoifanya katika Rukuu ndani ya Ibada ya Sala.Na imenukuliwa pia na Imam Abu Daud, Imam Ibn Majah, Imam Ibn Marduwayh, Imam Ahmad Ibn Hanbal n.k.

Na mbali ya maneno haya *Subhanah Rabbi Al Aadhiim* - Utukufu Kamilifu ni wake Mola wangu Mtukufu. Ambayo hutamkwa mara tatu katika Kila Rukuu ya Sala kama Sote tunaosali tunavyojua, lakini pia kuna Hadith isemayo kua : **'Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Qiyam Al Layl aliyarudia maneno haya katika Rukuu yake hadi Kikao chake kwenye Rukuu hio Kikafikia urefu wa Kisimamo chake pale anapokua anasoma Sura ndefu tatu kama Al Baqara na An Nisaa, na Al Imran kwani Sala yake hio ilikua Imejaa Dua na Istighfar.'**

Na Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akipenda sana kusema *Subhanaka Allahuma Rabbana Wa Bihamdika Allahuma Ighfir li* kila anaporukuu na kusjudu'***(Sahih Bukhari)***

Na anasema Imam Abu Daud kua:

حَدَّثَنَا مُسَدَّدٌ، حَدَّثَنَا خَالِدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، حَدَّثَنَا سَعِيدٌ الْجُرَيْرِيُّ، عَنِ السَّعْدِيِّ، عَنْ أَبِيهِ، أَوْ عَنْ عَمِّهِ، قَالَ رَمَقْتُ النَّبِيَّ ﷺ فِي صَلاَتِهِ فَكَانَ يَتَمَكَّنُ فِي رُكُوعِهِ وَسُجُودِهِ قَدْرَ مَا يَقُولُ " سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ " . ثَلاَثًا

Amesema Musadadu kua amesema Khalid Ibn Abd Allahi kua amesema Said Al Jurayriyu kuaamesema Said ku amemsikia Baba yake au Ami yake akisema: 'Mimi nimeshuhudia wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisali alikua akikaa katika hali ya Kurukuu na Kusujudu kwake kwa urefu wa kiasi ya mtu kua ni mwenye kusema*Subhanah Allahi wa Bihamdihi* mara tatu'

Na anasema Bahr ul ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifunua Pazia la Dirisha lake na akawaona Watu wanasali nyuma ya Abu *Bakr Radhi Allahu Anhu.* Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Hakuna kitakachobakia katika Ubashirio mwema wa Utume, isipokua Muono ambao Muislam atauona au Mtu mwengine atajaaliaa kuuona kwa ajili yake. Na Oneni kua Mimi nimekataza kusoma Qur'an wakati mtu akiwa katika Kurukuu au kusujudu. Kwani kuhusiana na Rukuu basi Mtukuzeni *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu ndani yake. Na katika kuhusiana na Sujud basi kueni na Ikhlasi katika Kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwani katika sehemu hio ya Sujud ndio Dua zenu Hujibiwa***(Sahih Muslim)***

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi katika Al Tahqiq kua: '**Katika Rukuu hua inapendekezwa kuongezea wa *Bihamdihi* kwa kusema *Subhanah Rabbi Al Adhiim wa bi Hamdi.***' Na huo pia ndio mtizamo wa Al Muhaqiq Imam Ibn Hajar Al Haytam na pia alivyofafanua Imam Al Khatib Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shibrini katika *Al Mughni Al Muhtaj na katika Tuhfah Al Muhtaj.*

Imam An Nawawi akasema pia kua: '**As-hab wetu katika Madhhab yetu wanasema kua:'Ni Sunna kusoma *Subhana Rabbiyal' Adhimi wa Bihamdihi.* Miongoni mwa wanazuoni waliotoa maandiko juu ya Sunna wakisema wa bihamdihi ni Al Qadhi Abu Thayyib, Al Qadhi Hussen, mwandishi wa kitabu Shamail, Imam Abu Hamid Al Ghazali na wanazuoni wengine.''**

Kisha Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: **'Hukmu hii ni yenye kutokana na Uthibitisho wa Hadith ya Uqbah Ibn Amir *Radhi Allahu Anhu*ambae amesema kua**;***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua kila anaporukuu basi husema: *Subhanah Rabbi Al Adhiim wa Bi Hamdihi* mara tatuNa kila anaposujudu basi husema *Subhanah Rabbi Al Aala wa Bihamdihi* mara tatu.'***(Sunan Al Kubra Al Bayhaqi na Imam Abu Daud)***

Ambapo ingawa Imam An Nawawi mwenyewe amesema kua Hadith hii kwenye Sanad yake kuna Rajul an Qawmihi yaani Mtu asietajwa jina kwa watu wake na hivyo kuifanya Hadith hii kua Majhul yaani asiethibitishwa katika mnyororo wa upekewaji wake lakini hata hivyo Imam Siraj Ad Din Abu Hafs Umar Ibn Ali Ibn Ahmad Ibn Mulaqin Al Shafii Al Masri amesema kua; '**Mtu huyo alienukuu ambae An Nawawi amesema hajulikani basi Ukweli ni kua ni Iyas Ibn Amir.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Al Hafidh Jamal Ad Din Abu Al Hajjaj Yusuf Ibn Zaki Abd Rahman Ibn YusufIbn Abd Al Maliki Yusuf Al Qalbi Al Qudha Al Mizzi basi yeye amesema kua **Mtu huyo si mwengine bali ni Iyas Ibn Amir'**

Na kwa upande wa Imam Ibn Hibban basi mesema kuhusiana nae kua: '**Iyas Ibn Amir huwa Min thiqat Al Misriyin yaani Ni Mtu mwenye Ilm nzito sana na inayoaminika ya Hadith miongoni mwa Wanazuoni wa Hadith wa Misri.'**

Na Imam Al Hakim Al Nishapuri Al Shafiii amesema kua: **'Iyas Ibn Amir ni Mwenye Sifa ya kua na Mustaqim Al Isnad yaani Nukuu zake ni zenye Misimamo yenye kuaminika.'**

Kwani kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: **'Ni Wajib kusema *Subhanah Rabbi Al Adhiim* mara tatu katika Rukuu na haitakiwi kuongeza chengine chochote.'**

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imama Malik basi wao Mtizamo wao ni kua: **'Ni wajibu kusema mara tatu *Subhanah Rabbi Al Adhiim wa Bihamdihi* au kusema *Subhanah Rabbi Al Adhiim**.'***

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi mtizamo wao juu ya hili ni kama wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal yaani inapendekezwa Kusema *Subhanah Rabbi Al Adhiim* tu basi.

Kwani tunapoangalia pia kwa upande mwengine basi tunaona pia kua amesema *Ummu ul Muuminina* Aisha *Radhi Allahu Anha*kama ilivyosema Hadith:

أَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ مَسْعُودٍ، قَالَ حَدَّثَنَا خَالِدٌ، وَيَزِيدُ، قَالاَ حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، عَنْ مَنْصُورٍ، عَنْ أَبِي الضُّحَى، عَنْ مَسْرُوقٍ، عَنْ عَائِشَةَ، قَالَتْ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يُكْثِرُ أَنْ يَقُولَ فِي رُكُوعِهِ وَسُجُودِهِ " سُبْحَانَكَ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي " .

Ismail Ibn Masoud amesema kua Khalid kua amesema Yazid, kua amesema Shu`bah kua amesema Mansour, kua amesema Abu Ad-Duha, kua amesema Masruq, kua amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua:*'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua mara kwa mara anaporukuu na anaposjudu hua ni mwenye kusema:*Subhanaka Allahuma Rabbana wa bi Hamdika, Allahuma Ighfrili* - Utukufu Uliokamilia ni wako Ewe Allah, na Shukrani zote unstahiki wewe Allah na Nakuomba nisamehe'*(*Sahih Bukhari)*

Ambapo ndani yake Hadith hii tunaona kua imetaja neno *Wa Bihamdi* ambalo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wameliona ni bora zaidi katika *Subhanah Rabbi Al Adhiim..Wabihamdi* kwani pia limenukuliwa kwenye Hadith tuliyoiangalia ya Uqba Ibn Amir. Na pia hadith hii ya Aisha *Radhi Allahu Anh*a inathibitisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua pia kwenye Rukuu.

Kama pia anavyosema Jabir Ibn Abdullah *Radhi Allahu Anhu katika* hadith ifuatayo:

أَخْبَرَنَا يَحْيَى بْنُ عُثْمَانَ الْحِمْصِيُّ، قَالَ حَدَّثَنَا أَبُو حَيْوَةَ، قَالَ حَدَّثَنَا شُعَيْبٌ، عَنْ مُحَمَّدِ بْنِ الْمُنْكَدِرِ، عَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم كَانَ إِذَا رَكَعَ قَالَ " اللَّهُمَّ لَكَ رَكَعْتُ وَبِكَ آمَنْتُ وَلَكَ أَسْلَمْتُ وَعَلَيْكَ تَوَكَّلْتُ أَنْتَ رَبِّي خَشَعَ سَمْعِي وَبَصَرِي وَدَمِي وَلَحْمِي وَعَظْمِي وَعَصَبِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

Yahya Ibn Uthman Al Homsi amesema kua Abu Haywa amesema kua Shuaib amesema kua Muhammad Ibn Al Munkadir, amesema kua Jabir Ibn Abdullah*Radhi Allahu Anhu,* Kua Alikua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaporukuu, hua ni mwenye kusema: "Ewe Mola wangu, ninapiga magoti Kwako, na kwako nimekuamini, na nimejisalimisha kwako, na kwako ninakutegemea wewe ni Mola wangu Mlezi katika kuona kwangu, na damu yangu, na nyama yangu, na mifupa yangu, na mishipa yangu, vinanyenyekea kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* , Mola Mlezi wa walimwengu wote."*(*Sunan An Nasai)*

Na kwa maana hio basi wacha tuainishe sehemu ambazo zinatumika Kuomba Dua ndani ya Sala.

Kwani anasema Mujaddid Ad Din Al Hafidh Imam Ibn Hajar Al Asqallani kua: '**Imethibitishwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua katika sehemu Sita, ambapo ndani yake tunaweza tukaongeza na mbili.**

1-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua baada ya *Takbirat Al Ihram* kwa kusema:

اللَّهُمَّ بَاعِدْ بَيْنِي وَبَيْنَ خَطَايَايَ كَمَا بَاعَدْتَ بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ، اللَّهُمَّ نَقِّنِي مِنَ الْخَطَايَا كَمَا يُنَقَّى الثَّوْبُ الأَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ، اللَّهُمَّ اغْسِلْ خَطَايَايَ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ

Allahumma baaid bayni wa bayna Khatayaayaya kama baaidta Bayna Al Mashriq wa Al Maghrib; Allahuma Naqqini Min Khataayaya kama yunaqqa al thawb al abyadh min Danas, Allahuma Ighsilni min Khataayaaya bi Althalj wa al Mai Al Barad -

Tafsir: ***Ya Allah tenganisha kiumbali baina yangu na Dhambi zangu kama ulivyotenganisha baina ya ukubwa wa Mashariki na Magharibi, Ya Allah nisafishe mimi kutokana na Dhambi kama inavyosafika Nguo nyeupe kutokana na UchafuYa Allah nikoshe Dhambi zangu kwa Theluji, Maji na Barafu****(Sahih Bukhari)*

2-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akikua akiomba Dua ndani ya Rukuu kwa kusema:

سُبْحَانَكَ اللّٰهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ، اَللّٰهُمَّ اغْفِرْ لِيْ

Subhanaka Allahuma Rabbana wa Bihamdika Allahuma Ighfir li.

3-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua baada ya Kutoka kwenye Rukuu na kusimama kwa kusema:

Sami Allahu Liman Hamida Allahuma Rabbana laka Al Hamd Mil-un Samawati wa Mil-un Al Ardh wa Mil-un Ma shiita min Shayn Baaid Allahuma Tahhimi bi al thalj, wa baradi wa Al Mai Il Baarid.

*Tafsir:****Allah anamsikia anaemsifu, Ya Allah, ewe Mola wetuKwako wewe ndiko kwenye Umiliki wa wa Sifa Tukufu zinazojaza Mbingu, zinazojaza Ardhi na zinazojaza chochote kile utakachozitia ndani yake. Ya Allah nikoshe kwa Theluji, kwa Maji ya Baridi na Barafu. (****Kama ilivyosema kwenye Hadith ya Ibn Abi Awfa Radhi Allahu Anhu)*

4-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua katika Sujud, ambapo hapa ndio alikua akiomba sana Dua.

5-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua Baina ya Sijda Mbili.

6-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua baada ya Tahhiyat ya Mwisho.

7-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua ya Qunut.

8-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua kila mara anaposoma Aya yenye Rehma kuomba Rehma hio na anaposoma aya ya Adhabu kuomba Kuepushwa na Adhabu hio*(Fat-h al Barr)*

Naingawa Hadith ya Uqbah Ibn Amir *Radhi Allahu Anhu* imesema kua; '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua kila anaporukuu basi husema: *Subhanah Rabbi Al Adhiim wa Bi Hamdihi* mara tatu.Na kila anaposujudu basi husema *Subhanah Rabbi Al Aala wa Bihamdihi* mara tatu.'** *(Sunan Al Kubra Al Bayhaqi na Imam Abu Daud)*

Lakini hata hivyo kwa upande mwengine basi hata kusema Dhikr hizo mara moja hua hakubatilishi Sala na hua inakubalika na kusema mara tatu au mara tano au mara saba.Na hii hua ni kulingana na Khushuu ya mtu ndani ya Moyo wake na hivyo pia Malipo ya Idadi yake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni kulingana naKhushuu na wingi wa Idadi ya Dhikr. Kwa maana hio basi kila ukisema kwa wingi zaid hua ni bora zaidi kimalipo.

Kwani Amesema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua: **'Mwenye Kusali anaweza kusema *Subhanah Rabbi Al Aadhiim* mara tatu katika Rukuu na hii hua ni kwa kiwango cha chini lakini hata akisema mara moja basi hua inatosha'***(Al Mughni)*

Na kwa upande wa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* basi yeye alisema kuhusiana na Amir ul Muumini Umar Ibn Abd Al Azizi *Radhi Allahu Anhu* kua:'**Hakika mimi sikuwahi kuona Sala ya mtu inayofanana na *Sala ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama Sala ya kijana huyu (Umar Ibn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhu)* Kwani nnadhania kua anasema *Subhanah Rabbi Al Adhiim* mara Kumi katika Rukuu na *Subhanah Rabbi Al Aala* mara kumi katika Sijda.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi yeye amesema kua: **'Amesema Hasan Al Basr kua: Njia Kamilifu ya Kusema *Subhanah Allah Al Adhiim* na *Subhanah Rabbi Al Aala* katika Rukuu na Sijda ni mara Saba au mara tano au mara tatu'**

Na akasema Imam Ash Shawqani kua: '**Hakuna Ushahidi kuhusiana na Ubora wa Idadi ya Tasbihi *(Subhanah Rabbi Al Adhiim, Subhanah Rabbi Al Aala)* katika Rukuu na Sujud bali mtu anatakiwa Afanye Tasbih kwa mara nyingi zaidi kwa kadri atakavyoweza kulingana na urefu wa Rukuu na Sijda ya Sala bila ya kijiwekea mipaka ya kiidadi na hakuna ushahidi wa kua mtu aseme kwa namba ya witri au zaidi ya mara tatu.'**

Kwa maana hio basi Kufanya Tasbih ndani ya Rukuu ya Sala hua kunategemeana na Sala, yaani kwa mfano Mtu akiwa anasali peke yake basi anaweza kufanya Tasbih kwa idadi atakayo, ingawa kulingana na Hadith ya Uqba *Radhi Allahu Anhu* tunaona kua Sunna ni kuanzia Mara tatu na hii pani kutokana na Hadith Ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: **'*Allah Subhanah wa Ta'ala* anapenda vilivyo katika ida ya Witr'***(Imam Bukhari).*

Na kama Mtu anasali nyuma ya Imam basi pia idadi Tasbih zake hua zitategemeana na Rukuu ya Imam, yaani kama ikiwa Rukuu ya Imam ni fupi basi na Tasbihi za Maamuma zitakua kidogo kiidadi, na kama Rukuu ya Imam Itakua ndefu basi na Tasbih za Maamuma zitakua nyingi.

Na Wanazuoni Wanasema kua '**Hata kama itakua umepoteza Idadi ya Tasbih katika Rukuu yako kutokana na wingi wake, basi Sala yako hua haijabatilika'***(Nur Al Idah, mam Ali Al Shurunbulali).* Kwa hivyo zimwage Tasbih kwa Kadri utakavyoweza kwa ajili ya kuiboresha Sala yako na kuvuna Malipo zaidi.

Kwani ingawa kwa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Ahmad Ibn Hanbal, Imam Abu Hanifa na Imam Malik na wengi Miongoni mwa Wanazuoni basi tunaona kua Tasbih katika Rukuu yaani Kusema *Subhanah Rabbi Al Adhiim wa Bihamdihi* hua ni Sunna.

Lakini kwa Upande wa Mwanafunzi wa Imam Muhammad Idris Al Shafii aliesoma pamoja na Imam Ahmad Ibn Hanbal chini ya Imam Al Shafii ambae ni Mwanazuoni mahiri wa Madhhab ya Imam Al Shafii katika Ardhi ya Khurasan aitwae Imam Is-haq Ibn Rahawayh Al Khurasani Al Shafii ambae pia na rafiki yake Imam Ahmad Ibn Hanbal basi yeye anasema kua: '**Tasbih hua ni Wajib, hivyo kama mtu ataachana nayo kuitamka kwa makusudi, basi Sala yake hua ni yenye kubatilika, lakini kama ataiwacha kwa kusahau basi haitobatilika.'**

Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal mwenyewe, kwani anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Tasbih Katika Rukuu,katika Sujud, kusema *Sami Allahu Liman Hamida* na Dhikr baina ya Sijda mbili na Takbir zote hua ni Wajib**. **Hivyo kama ukiziwacha kwa makusudi basi Sala yako ni Batil lakini kama ukiziwacha kwa kusahau basi haibatiliki ila itakubidi kuleta Sijda sahw.'**

Na huo pia ndio Mtizamo wa Imam Ibn Khuzaima.

Na anasema *Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din* Imam Abu Zakaraiyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Wanazuoni wa Jamhuri ya Madhhab ya Shafii Maliki na Hanafi wanakubaliana kua Kusoma Tasbih katika Wakati wa Kurukuu na Kusujudu hua ni Sunna na Wala si Wajib**. **Hivyo Mtu asipoisoma, au atakapoiwacha kwa Makususi ama kwa kusahau basi Sala yake haibatiliki jambo ambalo ni tofauti na upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ambao wao wanasema kua kusoma Tasbih huku ukiruku na kusuju hua ni Wajib'(***SharhAl Muhadhdhab)*

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: **'Hivyo Kusoma Tasbih na Dhikr nyengine katika wakati wa Kurukuu na Takbira zisizokua Takbirat Al Ihram, hua ni Sunna na hivyo Mtu akiiwacha kwa makusudi au kwa kusahau basi Sala yake inabakia kua Sahih, haibatiliki ila hua ni Makruh kuiwacha kwa makusudi. Na huo ndio Mtizamo wetu na ndio mtizamo wa Malik na Abu Hanifa na wengi miongoni mwa Wanazuoni'***(Al Majmuu)*

Na anasema pia Imam Yahya Ibn Abi Al Khair Al Imrani Al Shafii katika *Bayan Fi Fiqh Al Imam Al Shafii* kua: '**Na wala si Wajib kufanya Tasbih katika Rukuu wala katika kusujudu bali ni Sunna na huu ndio Mtizamo wa Wanazuoni wengi Sana.Na hii ni kwa sababu *Allah Subahnah wa Ta'ala* amesema katika Qur'an kua:**

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ امَنُوا ارْكَعُوا وَاسْدُدُوا وَعْبُدُوا رَبَّكُمْ وَافْعَلوا الْخَيرَ لَعَلَّكُمْ تُفَلِي﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona *(Surat Al Hajj 22:77)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini Rukuuni na Sujudini(Salini) na Muabuduni Mola wenu tu na fanyeni Amali njema ili mpate kufuzu hapa (Duniani na Akhera)***

Ambapo Ayah hii haikutaja Tasbihi ya aina yeyote ndani yake, na hivyo kukosekana kwa Tasbihi hakuwezi kubatilisha Sala, na *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* hakuamrisha Tasbihi katika Rukuu wala Sujudu.'

Kwa maana hio basi tunamalizana na Tasbih ya Rukuu kwa kuambiana kuaTasbih ya Ndani ya Rukuu ya *Subhanah Rabbi Al Adhiimu* hua ni Sunna, ambayo unaweza kuisema kuanzia mara moja au mara tatu lakini inapendekezwa zaidi kua uiseme kuanzia mara tatu na kuendelea zaidi kiidadi kwani kutaipandiasha Juu zaidi kidarja Sala yako mbele ya *Allah Subhabah wa Ta'ala.*

Na kwa kua ni Sunna na si Wajibu basi hata kama Mtu ukiisahau basi hua hamna tatizo kwani Sala yako haibatiliki na itakua Sahih, na kuiwacha pia hakuna tatizo ila kutapunguza Uzito wa Sala yako mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ndio Maana ikawa ni Makruh yaani Inakirisha kuiwacha kwa Makusudi.

UKAMILIFU WA RUKUU

❖❖❖

Na ingawa amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliingia Ndani ya Al Kaabah na (akasali na) Macho yake hayakuondoka kutoka kwenye Sehemu ya Kusjudia hadi pale alipotoka.'***(Imam Ibn Hibban)*

Ambapo hii ni Hadith inayothibitisha kua Mtu unaopokua katika Sala basi Macho yako yanatakiwa yawe yanatizama katika Sehemu unayosujudia.Na huo ndio Mtizamo wa Masahaba, wa Maimam wengi wakiwemo Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Hasan Al Basr, Imam Muhammaf Ibn Sirrin n.k na pia ndio Mtizamo wa Madhhab yote.Kwani Imam Abu Qilaba anasema kua: **'Mimi nilimuuliza Muslim Ibn Yassar**: '**Hivi Jee macho yangu yaangalie wapi katika wakati nnaosali?'**

Muslim Ibn Yassar akajibu: Yatupie katika Sehemu unayosujudia hivyo ndio bora kwako'.

Na amesema Abd Allah Ibn Al Zubayr *Radhi Allahu Anhu* kua: **Wakati *Rasul Allah Salallaju Alayhi wa Salam* alipokua akikaa Attahiyat basi alikua akiweka Mkono wake wa Kushoto kwenye Paja lke la kushoto, na mkono wa kulia kwenye Paja la kulia na alikua akinyoosha kidole chake cha Shahada huku mtizamo Wa Macho yake ukiwa hauvuki zaidi ya kidole hicho.'***(Imam Abu Daud)*

Kwani hio ni kuhusiana na Mtizamo wa Jicho katika Sala kwa Ujumla, na pia uthibitisho wa mipaka ha Mtizamo wa jicho katika Wakati wa Attahiyat. Na hivyo anasema Imam An Nawawi kua: 'Ni Sunna kutoruhusu Mtizamo wa Jicho kutotizama sehemu nyengine zaidi ya Kidole cha Shahada.'*(Sharh Sahih Muslim)*

Ila Suali linakuja, Hivi jee katika Rukuu inatakiwa Mtizamo wa Jicho uwe unaangalia wapi?Naam kuhusiana na jibu la suali hili basi anasema Al Faqih Al Imam Abd Al Hamid Al Sharwani Al Shafii katika *Tuhfah Muhtaj Sharh Minhaj* kua: '**Kwa Mujibu wa Mtizamo mwengine Ndani ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua Mtu mwenye kusali anatakiwa atizame katika sehemu ya Kusjudia katika wakati akiwa katika Qiyyam (Kisimamo)'**

Na anatakiwa aangalie kuelekea katika Nyayo za Miguu katika Wakati anaporukuu.

Mtizamo wake uwe ni wenye Kuelekea Puani katika Wakati wa Kusjudu.

Mtizamo wake uwe ni wenye kuangalia Mapajani, Magotini katika Wakati anapokaa Attahiyat.Na hii ni kwa sababu kurefusha Mtizamo wa Macho hua kunaweza kupelekea kuvuruga Umakini ndani ya Sala ya Mtu husika.

Hivyo kama Mtu anaesali katika wakati wa Kurukuu atakua ni mwenye kuangalia katika sehemu iliyokaa Nyayo za Miguu yake badala ya kuangalia katika sehemu anayosujudia basi kufanya hivyo itakua bora zaidi na muhimu zaidi. **Na huo pia ndio Mtizamo wa Imam Al Baghawi na Imam Al Mutawwali.'***(Tuhfah Muhtaj Sharh Minhaj)*

Hivyo basi mbali ya kua tunaposali tunatakiwa kuangalia katika Sehemu tunayosujudia lakini pia kwa upande mwengine basi hua inaruhusika katika wakati wa Kurukuu kuangalia katika sehemu zilizokaa nyayo zako, yaani kwenye sehemu uliyoweka Miguu yako kama kufanya hivyo kutakupa umakini zaidi.

Ama tunapozungumzia kuhusiana na kuiwahi Rukuu ya Imam katika Sala ya Jamaa, basi amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

Yeyote yule atakaeiwahi Rukuu ya Imam basi hua pia ni mwenye kuiwahi Rakaa.'*(Imam Abu Daud)*

*Na amesema Abd Allah Ibn Masud Radhi Allahu Anhu kua: '***Yeyote yule ambae hakumuwahi Imam katika Rukuu basi Hakuiwahi Rakaa'***(Imam Al Bayhaqi)*

Na amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Yeyote yule atakaemuwahi Imam Katika Kurukuu kwake kabla ya Imam Hajanyanyuka kutoka katika Rukuu hio basi hua ameiwahi Rakaa.'***(Imam Al Bayhaqi)*

Na akasema tena Abd Allah Ibn Umar*Radhi Allahu Anhu* kua:**'Kama utamuwahi Imam akiwa katika Rukuu na wewe ukawahi kuweka mikono yako kwenye magoti yako kabla Imam hajanyanyuka basi Umeiwahi Rakaa.'***(Mawsuah Al Fiqhiyya Al Quwaittiya)*

Na akasema Zayd Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Yeyote yule atakaeiwahi Rakaa kabla ya Imam hajanyanyua kichwa chake kutoka kwenye Rukuu basi hua ameiwahi Rakaa'***(Mawsuah Al Fiqhiyya Al Quwaittiya)*

Na hizi ni Hadith Sahih zinazozungumzia kuhusiana na Rukuu na Kuiwahi Rakaa katika Sala ya Jamaa ambazo zimejaa kwanye vitabu vya Hadith vya Imam Abu Daud, Imam Al Bayhaqi, Imam Ibn Khuzaymah, Imam Al Daraqutni, Imam At Tabarani, Muwatta Imam Malik, Imam Ibn Ani Shaybah na Imam Ibn Abd Razzaq.

Abmbapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Ramli kuhusiana nazo kua: '**Maneno yasemayo Kama Maamuma ataiwahi Rukuu ya Imam basi hua ameiwahi Rakaa hua yanamaanisha kua:Kile alichokikosa Maamuma katika Sala yaani Kisimamo, Kisomo cha Surat Al Fatiha, na Kisomo chengine, basi hata kama ilikua Maamuma alivikosa bila ya kua na sababu ya msingi hata kama kwa uvivu tu basi hua ameipata Rakaa**, **Na hii ni kutokana na Uthibitisho wa Hadith isemayo, Yeyote yule atakaeiwahi Rakaa kabla Imam hajanyanyuka kutoka kwenye Rukuu basi hua ameiwahi Rakaa.'***(Nihayat Al Muhtaj)*

Na huo pia ndio Mtizamo wa Imam Al Muhaqqiqin Shaykh Islami Imam Ibn Hajar Al Haytami katika *Tuhfah Al Muhtaj bi Sharh Al Minhaj.*

Na ingawa nimewanukuu Wanafiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii lakini huu si mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii pekee kwani huu ndio Mtizamo wa MadhhabYote ambapo anasema Imam Ibn Hazim kua: **Wanazuoni wanakubaliana kua Yeyote yule atakaemuwahi Imam kabla hajanyanyua kichwa chake kutoka kwenye Rukuu, basi atakua ameiwahi Rakaa, na kama Mtu akimkuta Imam Ameshanyanyua Kichwa kutoka kwenye Rukuu basi Mtu huyo hua ameikosa Rakaa ya Sala husika***(Maratib Al Ijmaa)*

Ama kwa upande wa Salat Al Jumaa basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyiddin Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: '**Kama Maamuma akimuwahi Imam katika Rukuu ya pili ya Sala ya Ijumaa, basi Maamuma huyo atakua ameipata Sala ya Ijumaa**. **Na kama ikiwa atamkuta Imam ananyanyua kichwa kutoka kwenye Rukuu basi Maamuma hajaipata Sala ya Ijumaa na hivyo Imam atakapotoa Salam basi itambidi Maamuma huyo kunyanyuka na Kuendelea Kusali Rakaa Nne za Salat Adh Dhuhr.'***(Rawdah Talibin)*

Na Al Allamah, Al Qadhi Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii anasema pia kua: '**Kama Maamuma akiwahi Rakaa nzima ya Sala ya Ijumaa basi atakua ameiwahi Sala ya Ijumaa, lakini kama ikiwa hakuiwahi na amemkuta Imam ameshanyanyuka kutlka kwenye Rukuu, basi Maamuma huyo itambidi amalizie Sala hio kama Salat Adh Dhuhr badala ya kama Salat Al Jumaa'h.'***(Al Iqna)*

Na mtizamo huo pia umefafanuliwa na Imam Al Khatib Al Shirbini katika *Umdat Al Muftin.*

Ama tunapoangalia kuhusiana na Hukmu ya Takbir ya Maamuma aliemkuta Imam akiwa kwenye Rukuubasi Wanazuoni wametofautiana juu ya hili, ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kama Mtu akimkuta Imam yuko katika Rukuu, basi kwanza Mtu huyo anatakiwa aseme *Takbirat Al Ihram* (ya Kuingilia kwenye Sala) wakati akiwa amesimama, na kisha aseme Takbir ya Rukuu Huku akiwa Anarukuu**. **Kwani akisema Takbirat Al Ihram huku akiwa hajasimama basi Sala yake hua inahesabika kua ni Batili na haiwezi kuhesabika kama ni Sala ya Fardhi wala haiwezi kuhesabika kua ni Sala ya Sunna'***(Al Majmuu)*

Kwa maana hio basi Ukimkuta Imam yuko katika Rukuu basi itakubidi ufanye Takbirat Al Ihram wakati ukiwa umesimama katika Qiyam, na halafu unatakiwa Kufanya Takbir nyengine ya Kuingia kwenye Rukui ambayo pia hua ni yenye kuashiria kumfuata Imam kwenye Rukuu.

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua:**'Na Maamuma akimkuta Imam anasjudu, basi anatakiwa aseme Takbirat Al Ihram na kisha Moja kwa moja Asjudu, bila ya kusema Allahu Akbar nyengine.Na kuna waliosema kua Maamuma anatakiwa asema Allahu Akbar kama vile anavyotakiwa kusema pale anapomkuta Imam kwenye Rukuu yaani Takbir ya Kuruku.Na Mtizamo huu ni kwa sababu waliosema hivyo hawajui umuhimu wa Allahu Akbar ya katika Rukuu, kwani zinatofautiana, kwani Takbir ya kwenye Rukuu ndio uthibitisho wa Rakaa yake Maamuma, Jee huoni kua inatosheleza kua kama ingekua sio Wajibu basi Sala hio hua ni kama Sala ya Mtu peke yake?**'(*Al Majmuu*)

Hivyo hio ni kwa upande wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii ambapo tunapoangalia kwa upande wa Madhhab mengine basi tunaona kua wao wanasema kama ifuatavvyo:

Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Al Tahtawi kua: Hua haina haja kutamkwa Takbir Mbili yaani Moja ya Ihram na ya pili ya Rukuu, hivyo anaemkuta Imam amerukuu basi anasema Takbirat Al Ihram kisha anarukuu.

Na kwa Upande wa Imam Malik basi nao wanasema kua: Maamuma anapomkuta Imam amerukuu basi hua haina haja kwake kutamka Takbir mbili, bali hutakiwa kutamka Takbir moja tu kwa ajili ya Kuingia ndani ya Sala na Kurukuu hio hio.'

Na kwa Upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Al Allamah Al Imam Ali Ibn Sulayman Al Mardawi kua: 'Maamuma akimkuta Imam amerukuu basi anatakiwa ajiunge nae kwa Takbir Al Ihram tu na kisha arukuu bila ya kusema Allahu Akbar.Ingawa imetajwa kwenye Al Mughni na Al Sharh na kwengineko kua anatakiwa aseme Allahu Akbar mbili, lakini Imam Ibn Tamim na Imam Al Fayed amepinga hivyo.'

Lakini baadhi ya wanazuuoni wanaona kuwa sala itakua ni sahihi, na hiyo katika hili basi Takbira Moja hua inatosha, kama ilivyonukiliwa katika riwaya iliyotoka kwa Imam Ahmad.'

Kwani imepokewa kutoka kwa Imam Ahmad katika riwaya ya mwanawe Saleh ambae aliuliza: 'Hivi jee Atakayekuja na akamkuta Imam yuko katika hali ya kurukuu, na akasema takbira mara moja, itatosheleza ama la?'

Imam Ahmad akauliza: 'Je, alikusudia kuanza nayo ama la?

Imam Ahmad akaambiwa: 'Iwe Alikusudia au hakukusudia.'

Imam Ahmad akasema: 'Jee hakuja akiwa na ni ya kukusudia Kusali?!" Kwa sababu nia ya rukuu haipingani na nia ya Takbira Al Ihram; Kwa ajili hii, imeamuliwa kuwa anaingia kwenye Sala na Takbira ya ufunguzi katika hali kama hii.

Hivyo Mwenye kumkuta Imamakiwa katika rukuu, basi takbira moja inamtosheleza, nayo ni Takbira ya Ihramu, ambayo ni nguzo isiyoondolewa kwa hali yoyote ile, na Takbira ya rukuu imeondolewa hapa, na mtizamo huu pia umepokewa kutoka kwa Zaid Ibn Thabit*Radhi Allahu Anhu* na Abd Allah Ibn Umar*Radhi Allahu Anhu,* Na kwa sababu Fardhi mbili za aina moja zimeunganishwa katika sehemu moja, moja wapo ni sehemu muhimu na nyingine inaangushwa kwayo, kama vile mwenye kuhiji akifanya Tawaf ya Kuzuru alipotoka Makka, basi inatosha kwa ajili yake. Tawaf ya kuaga.

Ambapo wanaoounga mkono mtizamo huu basi hua wanatumia uthibitisho wa Hadith ya Zaid Ibn Wahab *Radhi Allahu Anhu* mbae amesema kua; **'Mimi nilitoka pamoja na Abd Allah Ibn Masud *(Radhi Allahu Anhu)*kutoka nyumbani kwake kuelekea Msikiti na tulipofika ndani katikati Msikitini basi Imam akarukuu kabla ya yetu sisi kuifikia safu ya Sala, na hapo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*akasema Takbir na kisha akainama katika kuruku. na mimi nikamfuata pia, na wakati tukiwa kwenye Rukuu tukatembea kujiunga na safu na tulipofika kwenye Safu tutakuta watu wananyanyua vichwa vyao kutoka kwenye Rukuu. hivyo Imam alipotoa Salam basi mimi nikajihesabu kua sijaiwahi Rakaa na nikanyanyuka, lakini Abd Allah Ibn Masud *(Radhi Allahu Anhu)* akaukamata mkono wangu na kunirudisha chini huku akiwa ni mwenye kuniambia kua: 'Uliiwahi Rakaa''**

Na pia kuna Hadith ya Abu Bakra *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:**'Mimi nilingia katika Sala wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa katika Rukuu, na hivyo nikaingia kwenye Rukuu kabla ya kuingia kwenye Safu ya Sala. na kusali, na baada ya kusali nikamwambia *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam juu* ya hili ambapo nae akaniambia: 'Namuomba Allah akuongezee mapenzi katika kufanya mema, lakini usirudie tena jambo hilo''***(Sahih Bukhari)***

Na ingawa Imam Al Mardawiyaliunga mkono mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal hapo awali lakini baadae amesema pia katika (Al Insaaf) kua:**"Lau ingekusudiwa kwa Takbira moja katika Ihram Takbir na Rukuu, basi Salah isingesaliwa kama inavyosaliwa kwa mujibu wa mafundisho sahihi.'**

Na tunaporudi kwenye Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ni kua unapomkuta Imam amerukuu nawe ukajiunga nae basi Useme Takbirat Al Ihram na Kisha Urukuu kwa Takbirat ya kurukuu basi tunaona kua anasema Imam Abu Daud kua: **'Mimi nilimuuliza Imam Ahmad Ibn Hanbal: Hivi Jee kutamka Takbirat Mbili ni bora kwako?Ambapo nae akasema: Naam, na mtu akitamka Takbira mbili basi hua hakuna kutokukubaliana juu ya hilo**.*(Masail Al Imam Ahmad)*

Kwa maana hio basi hua ni bora kufuata Mtizamo Wa Madhhab ya Imam Al Shafii katika hili na hii ni kwa sababu kusema Takbira mbili hua ni bora zaidi.

Hivyo wale Wanaosema kua kua Mtu atakaemkuta Imam amerukuu basi na yeye akijiunga nae anatakiwa afanye Takbirat Al Ihram tu ambayo hio hio ndio itakayotosheleza na kwenye Rukuu na hivyo arukuu basi ni wenye kusimamia kwenye Hadithi zifuatazo:

عن الحسن، أن أبا بَكْرَة جاء ورسول الله راكع، فركع دون الصَّف ثم مَشَى إلى الصَّف فلما قَضَى النبي صلى الله عليه وسلم صلاته، قال: «أيُّكم الذي ركع دون الصَّف ثم مَشَى إلى الصَّف؟» فقال أبو بَكْرَة: أنا، فقال النبي صلى الله عليه وسلم : «زادَك الله حِرْصَا ولا تَعُد».

Kutoka kwa Al Hasan ambae amesema kua: Abu Bakra alikuja Huku *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*(akiwa anasalisha) akiaa amerukuu. Hivyo Abu Bakra Akarukuu na kisha akaelekea kujiunga na Safu.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomaliza Kusali akauliza: Jee ni nani miongoni mwenu alierukuu kisha akaelekea kujiunga na Safu?**

Abu Bakra *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ni mimi hapa *Ya Rasul Allah'*

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema Allah akuzidishie bidii (katika Ibada zako) lakini usirudie tena.'(Imam Abu Daud, Musnad Imam Ahmad, Imam Al Bukhari)*

Naam..hadithi hii inatuonesha kua Abu Bakra *Radhi Allahu Anhu* aliingia Msikitini na akamkuta *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa anasalisha na yuko katika Kurukuu. Hivyo *Abu Bakra Radhi Allahu Anhu* alipoona hali hii na yeye yuko mbali kidogo na Safu na anataka kuiwahi Rakaa. Basi pale pale alipo akatia nia, akapika *Takbirat Al Ihram* na kisha akarukuu kabla hajaifikia Safu, na kisha akapiga hatua kuelekea kwenye Safu kwa ajili ya kujiunga na safu ya Sala ya Jamaa.Na hivyo akaendelea na kusali hadi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomaliza kusali akauliza ni nani aliefunga Sala na kurukuu kabla ya kuifikia Safu?

Na Abu Bakra *Radhi Allahu Anhu* akasema kua ni yeye, na *hivyo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akamjombea Dua kua aongezewe bidii katika kukimbilia Kufanya Amali njema, na kisha akamwambia kua asifanye tena hivyo kukimbilia Sala kwa sababu kufanya kwake hivyo hua kunamkosesha utulivu ndani ya Sala.

Ambapo uthibitisho wa Hadith nyengine ni ile ya Zayd Ibn Wahab ambae anasema kua:'**Mimi nilitoka pamoja na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kutoka nyumbani kwake kuelekea Masjid Tulipofika Msikitini tukakuta Imam amerukuu pamoja na Maamuma, hivyo hapo hapo Abd Allah Ibn Masud akafunga Sala na kurukuu, na mimi nikamfuata pia**. **Na wakati tukiwa kwenye Rukuu tukakimbilia kwenye Safu, na tulipofika kwenye Safu tukakuta Watu wananyanyuka kutoka Kwenye Rukuu, nasi tukanyanyuka na tukasali hadi Imam alipotoa Salam, basi mimi nikadhania kua ile Rakaa sikuipata**. **Hivyo nikanyanyuka kuja juu lakini Abd Allah Ibn Masud akanikamata mkono na kunirudisha chini na kusema: 'ile Rakaa uliiwahi'***(Imam Ibn Abi Shaybah)*

Naam..kwa kua katika Hadith ya kwanza tumeona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m hakumwambia Abu Bakra *Radhi Allahu anhu* kua airudie Sala yake,Na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*ambae ni miongoni mwa Masahaba wanazuoni kumkataza Zaid Ibn Wahab kua asiendelee kusali kwani ameiwahi Rakaa, na kwa kua hizi ni Hadith Sahih kulingana na vigezo vya baadhi ya Wanazuoni basi nao wanametoa Hukmu hio ndani yake kua Takbirat ya Ihram inatosha na hivyo kujumuisha pamoja na Rukuu pale inapotokea hali kama hii ndani ya Sala.

Ambapo hata hivyo huu si Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii,na ingawa Hadith hizi zimo kwenye Sahih Bukhari lakini Imam Al Bukhari mwenyewe amepingana na Mtizamo huo na kufuata Mtizamo

wa Imam Al Shafii usemao kua Mtu unatakiwa useme Takbira mbili ya Kuingilia kwenye Sala na kisha ya Kurukuu.

SIRI YA RUKUU

❖❖❖

Kwani mbali ya kua Rukuu ni Hatua ya Sala yenye kuonesha Heshima na Unyenyekevu wa Mja mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* lakini pia Adhkar zilizoko ndani yake hua ni zenye Siri kubwa sana kiasi ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anaposali Qiyyam Al Layl basi hutumia mda mrefu sana katika Rukuu huku akiwa ni mwenye kusema:

سبحان ربي العضيموبحمده

Subhanah Rabbi Al Adhiim wa Bihamdihi

Yaani: **Utukufu ni wake Mola wangu Mtukufu ambae ni pekee mwenye kustahiki Shukran**

Ambapo katika Kutamka neno *Subhanah* basi hua unamaanisha Kutangazia Utukufu uliokamilika usiokua na Mfano wake ambao ni wenye kutokua na kasoro yeyote.

Kwani unaposema *Subhanah Rabbi* basi moja kwa moja Utukufu huo hua unauianisha kua ni wa Mola ambae ni wako wewe unaemtukuza na hivyo hua ni mwenye kukupelekea hali yako hio kua ni yenye kukukaribisha karibu sana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa mpenzi, huruma na unyenyekevu Na hivyo hua ni mwenye Kukubali kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie Mola wako.

Ambae ndie alieuumba kila kitu na kukisimami atagu mwanzo wake hadi mwihso wake, ndie aliewalea wazee wako na akakulea wewe kabla ya kuzaliwa kwako, na baada ya kuzaliwa kwako kwa kukujaalia kila ulichokua ukikihitajia katika maisha yako hapa Duniani.Na ndie atakaekulea na kukusimamia hadi mwisho wa Maisha yako kesho Akhera na kukuhukumu kutokana na Amali zako ambazo ulizifanya kwa khiari yako.

Na katika kumtukuza kwako huko kupitia katika maneno haya *Subhanah Rabbi Al Adhiim* basi hua unadhibitisha pia kua kutokana na Ukamilifu wake kiutukufu basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hahitaji Msaada wa yeyote kwani yeye ni mwenye uwezo juu ya kila kitu, Kinguvu, Kiutajiri, Kimamlaka n.k

Hivyo kila Mtu unaporukuu basi unatakiwa ufaham kua Hio hatua ya kitendo uliyoitekeleza ndani ya Sala yako na Maneno unayoyasema katika wakati huo hua si maneno yanayotamkwa kimazoea tu, bali ni manemo yenye maana na uzito mkubwa sana kiasi ya kua yanahitaji Umakini na mazingatio yake kimaana na katika kuyatamka kwake, kwani unatakiwa uyahisi ndani ya Moyo wako katika Kuyatamka kwako, na hapo ndipo utakapohisi ladha ya Ibada ya Sala na ndipo utakaponufaika na manufaa ya Rukuu katika Sala.

Kwani anasema Mujaddid Ad Din, Hujjat Ul Islami Imam Al Shafii Al Thani, Zukhruf Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: '**Rukuu na Sujudu Ndani ya Sala katika Sala hua ni zenye kuurudisha Uthibitisho wa Uungu na Ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Kwani katika Kurukuu hua unarudia kuthibitisha Unyenyekevu wako na Kujisalimisha kwako, na kuonesha Jitihada za Kuboresha Hisia za Ndani kabisa ya Moyo na Mwili wako wako kupitia kwenye utambulisho wa kujitambua Udhaifu wako na kutokua na thamani yeyote kwako mbele ya Utukufu, Ukubwa na Ufalme wa Mola wako.Katika kuthibitisha kwako haya basi hua unatumia msaada wa Ulimi wako kumtukuza Mola wako na kurudia rudia kuthibitisha Mamlaka ya Ufalme wake'*(Ihya Ulum Ad Din)***

Kwa upande mwengine basi anasema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: **'Sijawahi mimi kumuona *RasulAllah Salallahu Alayhi wa Salam* akisali kama alivyokua akisali baada yakushushwa kwa Surat Al Nasr bila ya kusoma Dua isemayo:**

سُبْحَانَكَ اللّٰهُمَّ رَبَّنَا وَبِحَمْدِكَ، اَللّٰهُمَّ اغْفِرْ لِيْ

'*Subhanak Allahuma Rabbana wa Bi Hamdika Allahuma Ighfirli* - Utukufu ni Wako Ewe Allah Mola wetu unaestahiki shukrani zote, Ya Allah Nisamehe' katika Rukuu.'*(Sahih Muslim)***

Ambapo hii ni moja kati ya Hadith zinazotuonesha uzito na Thamani wa neno Subhanah Allah, kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akipenda kuitamka Tasbih hii mwishoni mwa Uhai wake ambapo baada yake hua ni mwenye kuomba Dua ya Msamaha kama ilivyomuamrisha aya hio ya Surat An Nasr iliposema:

﴿فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا﴾

***Fasabih Bihamdi Rabbikawa Istaghfirhu Innahu Kana Tawaban* - Kisha Mtukuze Mola wako kwa Sifa zake na Muombe msamaha kwani yeye Ni mwingi wa Usamehevu'**

Ambapo amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'*Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:'Maneno Mawili ni mepesi sana kwenye Ulimi, lakini ni Mazito sana kwenye Mizani na ni yenye kupendwa sana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni:**

سبحان الله وبحمدهسبحان الله العضيم

Subhanah Allahi wabihamdihi Subhanah Allahi Al Adhiim'*(Mutawafaq Alayhi)*

Na amesema tena Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Mwenye kusema *Subhanah Allah wa Bihamdihi* mara 100 kwa siku basi dhambi zake zote zitafutwa hata kama zitakua wingi wake kama povu la bahari.'** *(Mutawwafaq Alayhi)*

Na imenukuliwa kwenye hadith nyengine kua:

وعن أبي ذر الغفاري رضي الله عنه قال: قال رسول الله – صلى الله عليه وسلم –: «ألا أخبرك بأحب الكلام إلى الله؟». قلت: يا رسول الله! أخبرني بأحب الكلام إلى الله، فقال: «إن أحب الكلام إلى الله، سبحان الله وبحمده». (صحيح مسلم)

Na akasema Abu Dhar Al Ghifari *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Aliniambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema kua: Jee nikuambie ni Kauli gani inayopendwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala?'***

'Nami nikasema : Naam, ya *Rasul Allah* Niambie ni Kauli gani inayopendwa zaidi na *Allah Subhanah wa Ta'ala?'*

'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: *Subhanah Allah Wabihamdihi'(*Sahih Muslim)*

Na akasema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:'**

'Mwenye Kusema - *Subhanah Allahi Al Adhiim wa Bihamdihi* - Basi anapandiwa Mtende Peponi na *Allah Subhanah wa Ta'ala'*(*Imam At Tirmidhii)*

Na amesema tena Abu Dhar Al Ghifari *Radhi Allahu Anhu* kua:

أن رسول الله – صلى الله عليه وسلم – عاده، أو أن أبا ذر عاد رسول الله – صلى الله عليه وسلم – فقال: بأبي أنت وأمي يا رسول الله! أي الكلام أحب إلى الله عز وجل؟ قال: «ما اصطفى الله لملائكته: سبحان ربي وبحمده سبحان ربي وبحمده سبحان ربي وبحمده». (صحيح الترمذي)

'Alinitembelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nami nikamwambia: 'Baba yangu na Mama yangu watolewe Kafara kwa ajili yako ya *Rasul Allah!* Hebu niambie ni Kauli gani ambayo inapendwa zaidi na *Allah Subhanah wa Ta'ala*?'

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Yale maneno *a*liyowachagulia *Allah Subhanah wa Ta'ala* Malaika wake: *Subhanah Rabbi Wabihamdihi, Subhanah Rabbi Wabihamdihi, Subhanah Rabbi Wabihamdihi'*(*Imam At Tirmidhii)*

Naam, hivyo Maneno tunayoyasema Ummati wa Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* Ndani ya Rukuu ya Sala ni maneno waliyochaguliwa Malaika wayaseme.

Kwani anasema Imam Jafar As Sadiq ambae ni Mwalimu wake Imam Nuuman Ibn Thabit Abu Hanifa na pia mwalimu wa Imam Malik Ibn Anas ambae ni Mwalim wake Imam Muhamad Idris Al Shafii ambae ni Mwalim wa Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Hakuna Mja anaerukuu kwa Ikhlasi mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* Humpamba Mja huyo kwa Nuru yake Tukufu na Humfunika kwa Kivuli cha Ufalme wake na humvisha Vazi la Miongoni mwa Mawalii Waliochaguliwa nae.'**

'Kwani Rukuu hua ni Hatua ya kwanza ya Kumkaribia *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Sujud hua ni Hatua ya Pili ya kumkaribia *Allah Subhanah wa Ta'ala*Hivyo yule anaetekeleza ipasavyo hatua ya kwanza basi hua ni mwenye kustahiki malipo ya hatua ya pili.'

'Kwa sababu Rukuu hua ni Upole na Sujud hua ni Ukaribu. **Hivyo yule asiekua na Sifa Sahih hua kamwe hawezi kuifikia hatua ya Pili**. **Kwa maana hio basi Mtu unatakiwa Kuitekeleza Rukuu**

katika njia ya mtu mwenye Kujisalimisha kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Moyo wote, kwa Unyenyekevu na Khofu ya Ukubwa wa Mamlaka yake.'

'Na hivyo Mtu husika hua ni mwenye Kuinama kwa Unyenyekevu kwenye viungo vyake kama vile ambavyo Mtu anavyokua na woga na huzuni ya kua huenda akawa ni mwenye kukosa manufaa ya wale wenye kurukuu ipasavyo. **Hivyo ulinde Moyo wako kutokana na vishawishi, minong'onezo na mitego ya Shaytan**. **Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* humnyanyua Mja wake pale Mja huyo anapokua amejawa na Unyenyekevu na kua ni mwenye kujisalimisha mbele ya Mola wake kutokana na kujua Ukubwa na Uwezo wa Mola wake'**

Ambapo amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:Kwa Hakika wakati Mja anaposimama Kusali basi Dhambi zake huwekwa Juu ya kichwa Chake na Mabegani Mwake. Hivyo kila mara anapokua anarukuu au anasjudu basi Dhambi hizo huporomoka kutoka kwake'***(Sahih Ibn Hibban)*

Ambapo amesema Hudhayfah Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mimi nilisali na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Usiku Mmoja, na akaanza kusoma Surat Al Baqara, hivyo nikafikiria kua akifikia Aya ya 100 atasimama,Lakini akasoma na kuipita na nikadhania kua atasoma Surat Al Baqara yote ndani ya Rakaa Moja. Hivyo alipomaliza Kuisoma Al Baqara nikadhania kua Atarukuu lakini mara ghafla akaanza kusoma Surat Al Imran na alipoimaliza basi akaanza kusoma Surat An Nisaa.'**

***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma kwa Upole na kwa vituo kiasi ya kua alikua akifanya Tasbih na Dua kulingana na Mada ya aya husika. Baada ya Hapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akarukuu ambapo ndani ya Rukuu hio alikaa kwa mda mrefu sawia na mda aliokaa kwenye kisimamo cha Kisomo**. **Na kisha Akasjudu na pia ndani ya Sijda hio alikaa kwa mda mrefu sawia na mda aliokaa kwenye Kisimamo cha Kisomo**.(*Sahih Muslim)*

Kwani tunapoangalia mifano ya *Masahaba Radhi Allahu Anhum* katika Rukuu na Sijda zao ndani ya Sala zao, basi tunaona kua walikua wakifuata Mifano ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*katika Kufanya *Tasbih Subhabah Rabbi Al Adhim wa Bihamdihi na Subhanah Rabbi Al Aala Wabihamdihi* Nyingi zaid ndani yake.

Kwani anasema *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Kama mtu akitaka kuona namna alivyokua akisali *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* basi na amuangalie Abd Allah Ibn Masud katika Sala.'**

Ambapo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* amesema hivi kwa sababu Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* katika Rukuu za Sijda zake za ndani ya Sala alikua akitulia kwa mda mrefu sana kiasi ya kua hata Ndege walikua wanakuja na kutua juu ya mgongo wake kutokana na utulivu wa wakati akiwa kwenye Rukuu na Sujud zake.

Kwani anasema Imam Muslim Al Makii kua: '**Mara moja mimi nilimuona Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu* akiingia kwenye Rukuu, ambapo mimi nikasali na kusoma Surat Al Baqara, Al Imran, An Nisaa na Al Maidah, huku Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu* akiwa hajainua kichwa chake kutoka kwenyw Ruku**u.'*(Az Zuhd)*

Na akasema Imam Abu Muhamad Abd Allah Ibn Wahb Ibn Muslim Al Fihr anasema kua: '**Mimi nilimuona Sufyan Al Thawry katika Msikiti Mtukufu wa Makkah baada ya Salat Al Maghrib**

akisali Sala ya Sunna Ambapo ndani yake alisjudu bila ya kunyanyua kichwa kutoka kwenye Sijda hadi ilipoadhiniwa Adhana ya Sala ya Isha.'*(Siyar Nubula Al Aaalam)*

Na akasema Abu Qatn kua: '**Hakika mimi sikuwahi kumuona Shuubah Akirukuu isipokua hua ni mwenye kudhania kua amesahau kunyanyuka Na wala sijawahi kumuona akikaa baina ya Sijda mbili bila kudhania kua amejisahau.'***(Siyar Aalam Nubula)*

Ambapo anasema Abdaan kua: '**Hubdah Ibn Hakim alikua akifanya Tasbih ndani ya Rukuu na Sujud zaidi ya mara Thelathini.'***(Siyar Al Aalam Nubula)*

Kwani anasema Imam Sahl Al Tustari kuhusiana na wenye kutaka kua na Sifa za Kurukuu na Kusujudu ipasavyo ndani ya Sala kua: '**Kwa Hakika Moyo hua ni Kama Nyumba, kama haijakaliwa basi Huharibika na ikikaliwa na yule asiekua mwenyewe pia huharibika. Hivyo kama unataka Moyo wako Uwe Mzima na Imara basi usiruhusu Sala zako kua ni kwa yeyote isipokua kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee.'**

'Na ukitaka Kifua chako kiwe Imara Basi usiruhusu kitu chochote ndani yake isipokua kua na umakini na Akhera yako.'

'Na ukitaka kuudhibiti Ulimi wako basi usiruhusu Maneno yake yawe mengine yeyote isipokua Ukweli na Uaminifu.'

'Na ukitaka uzima wa Mwili wako basi usiuruhusu kufanya Matendo yeyote isipokua yale ya Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.' Naam..hizo ndio miongoni mwa Sifa za wenye Kurukuu kweli na kusujudu ipasavyo.

Ambapo kwa upande wa Uways Ibn Amir Ibn Juzay Ibn Malik Al Qarni Al Muradi Al Yamani ambae alikua ni Mcha Mungu aliekua akiishi katika Ardhi ya Yemen katika Wakati wa Uhai *wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* basi yeye alikua akichagua siku maalum ya kua ni siku ya kufanya Rukuu tu, kama alivyosema Imam Asbagh Ibn Zayd kua:

'Uways Al Qarni alikua kila siku inapoingia wakati wa Usiku hua ni mwenye kusema: Usiku huu wa Leo utakua ni kwa ajili ya Rukuu tu!Na kisha hua ni mwenye kukesha katika Usiku wa siku hio katika Rukuu hadi Alfajiri. **Na unapoingia Usiku wa Siku ya Pili hua ni mwenye kusema kua: Usiku huu wa leo utakua ni kwa ajili ya Kusujudu tu, na kisha hukesha katika Usiku huo akiwa kwenye Sujud tu**. **Na unapowadia Usiku wa Siku unayofuata husema kua Usiku huu wa leo itakua ni kwa ajili ya kutoa Sadaka tu, na hivyo hutoa sadaka kila kitu chake ndani ya Nyumba yake hadi iwe hamna kitu hata kimoja**. **Na kisha hunyanyua juu mikono na kusema Ya Allah usinilamu kwa alielala na njaa leo hii kwani mimi nimetoa chakula changu chote, na usinilauku kaa asiekua na nguo kwani nimetoa Nguo zangu zote,.nk.**

Ambapo amesema Imam Abu Nuaym katika Hilyat Al Awliyaa kua: '**Maana ya maneno yasemayo kua Uways hurukuu usiku kucha au Husujudu usiku kucha hua yanamaanisha kua Uways Al Qarni alikua anasali Sala ya Sunna kisha ndani yake anazirefusha Rukuu au Sujudu zilizomo ndani ndani yake.'**

Yaani anazirufusha kwa urefu sana kiasi ya kua Sala hio ya Rakaa mbili hua ni yenye kuanzia Baada ya Isha hadi Alfajiri.

Hivyo Tunamalizana kuhusiana na Nguzo ya tano ya Sala ambayo ni Rukuu kwa kukumbushana kua:

Miongoni mwa Manufaa ya Rukuu kama itatekelezwa ipasavyo kwa Afya ya Miili yetu basi hua ni yenye kusaidia kuongeza Mzunguko wa Damu ndani ya Ubongo, Kuulainisha mwili na pia Kuimarisha Misuli ya Kiuno na kuondoa Matatizo ya Maumivu ya Kiuno kutokana na Kuinama katika Kurukuu na kuinuka katika kufanya I'tidal.

6-ITIDAL AL QAWMA KISIMAMO CHA BAADA YA RUKUU

❖❖❖❖

Naam, tunaingia kwenye Nguzo ya Sita ya Sala ambayo ni yenye kuhusiana na kitendo kinachofuata baada ya kutoka kwenye Hatua ya Kurukuu na kabla ya Kuingia kwenye Hatua ya Kusujudu, yaani Kisimamo kilichopo baina ya Rukuu na Sujud au Itidal.

Ambapo neno I'tidal kwa kilugha hua linamaanisha Kua Na hali ya Kati na kati baina ya hali mbili tofauti, kua na msimamo usiofungamna na upande wowote, kua katikati baina ya pande mbili tofauti.
Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na I'tidal katika Ibada ya Sala basi hua tunamaanisha Kitendo cha Kutulia baina ya Nguzo mbili za Sala ambazo ni Rukuu na Sujud.Ambapo kitendo chenyewe cha I'tidal hua pia ni chenye kuhesabiwa kua ni Nguzo ya Sala.

Kabla ya kuendelea basi labda kidogo tufafanue kuhusiana na maana ya I'tidal kwa Ujumla katika Uislam.Na hii inabidi tukumbushane ni kwa sababu I''tidal ndio moja kati ya Sifa kuu za Dini ya Kiislam.

Kwani Dini ya Kiislam ni Dini isiyokua na Misimamo Mikali na waa isiyokua na Misimamo Regevu.
Na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema katika Qur'an kuhusiana na haya pale aliposema katika Qur'an kua:

﴿وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطاً لِّتَكُونُواْ شُهَدَآءَ عَلَى ٱلنَّاسِ وَيَكُونَ ٱلرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيداً وَمَا جَعَلْنَا ٱلْقِبْلَةَ ٱلَّتِي كُنتَ عَلَيْهَآ إِلاَّ لِنَعْلَمَ مَن يَتَّبِعُ ٱلرَّسُولَ مِمَّن يَنقَلِبُ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ وَإِنكَانَتْ لَكَبِيرَةً إِلاَّ عَلَى ٱلَّذِينَ هَدَى ٱللَّهُ وَمَا كَانَ ٱللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَانَكُمْ إِنَّ ٱللَّهَ بِٱلنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ﴾

Waka<u>dha</u>lika jaAAaln<u>a</u>kum ommatan wasa<u>t</u>an litakoonoo shuhad<u>a</u>a AAal<u>a</u> alnn<u>a</u>si wayakoona alrrasoolu AAalaykum shaheedan wam<u>a</u> jaAAaln<u>a</u> alqiblata allatee kunta AAalayh<u>a</u> ill<u>a</u> linaAAlama man yattabiAAu alrrasoola mimman yanqalibu AAal<u>a</u> AAaqibayhi wa-in k<u>a</u>nat lakabeeratan ill<u>a</u> AAal<u>a</u> allad<u>dh</u>eena had<u>a</u> Allahu wam<u>a</u> k<u>a</u>na Allahu liyud<u>dh</u>eeAAa eem<u>a</u>nakum inna Allaha bialnn<u>a</u>si laraoofun rah<u>h</u>eemun*(Surat Al Baqara 2:143)***

Tafsir: ***Na Kadhalika pia Tumekujaalieni (Nyinyi Waislam) kua ni Ummah wa Kati na KatiIli Muwe Mashuhuda kwa WatuNa pia Awe Mtume(Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam)Shahidi juu yenu. Na tulikifanya Qiblah ambacho mlikua mkikielekea kwa ajili ya kuwajaribu wale ambao ni wenye kumfuata Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam na wale watakageuka. Kwa hakika ni kuzito sana isipokua kwa wale ambao Allah Subhanah wa Ta'ala amewaongoza na Allah Subhanah wa Ta'ala hatozifanya Amali zenu kua ni zenye kupotea, kwani kwa hakika Allah Subhanah wa Ta'ala kwa Watu ni mwingi wa Rehma.***

Hivyo aya inatubainishia kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametujaalia sisi Waislam kua na sifa ya kua ni Ummah ambao ni Mfano wa Kuigwa kwa wengineo.Ambapo Neno Wasat lililotumika hapa pia hua linamaana sawa na maana ya neno I'tidal.

Ambapo kwa upande mwengine basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameyasema haya kwa sababu Umma wa Kiislam ni Ummah, uliopo baina ya Ummah za Imani mbili tofauti ambazo ni za Kiyahudi na Kikriisto.

Kwani kwa upande wa Mayahudi basi wao walivuka mipaka ya Maamrisho ya Mola wao kwa kuwachinja Mitume wao na Wanazuoni wao.

Na kwa upande wa Wakristo wakivuka mipaka ya Maamrisho ya Mola wao kwa kutangazia kua Isa Ruhi Allahi kua ni Mtoto wa Mungu.

Ambapo Waislam ni wenye sifa ya Kushikamana na Maamrisho ya Mola wao na kuachana na Makatazo ya Mola wao.

Ambapo anasema Abu Said Al Khudri kua**: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Katika Siku ya Malipo Kuna Mtume atakuja na Mtu mmoja, na kuna Mtume atakaekuja na watu wawili na kadhalika. Kisha watu hao wataulizwa Jee Mtume wenu alikufikishieni Ujumbe.'**

'Nao watasema La!'

Hivyo Mtume wao ataulizwa: 'Jee uliwafikishia Ujumbe?' Ambapo nae atasema: 'Naam!'

Mitume hao wataulizwa: 'Jee ni nani atakaetoa Ushahidi Juu yenu leo hii(kua kweli Mlifikisha Ujumbe)
Mitume hao watasema: 'Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam atatoa Ushahidi na Ummah wake pia utatoa ushahidi.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Ummah Ummah wake utaitwa na Kuulizwa: 'Hivi Jee Mtume huyu aliufikisha Ujumbe wa Mola wake kwa Watu wake?'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Ummah wake utasema: 'Naam! Ndio alifikisha.'**

***Allah Subhanah wa Ta'ala* atauuliza Ummah wa*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na: 'Jee Mmejuaje Nyinyi?'**

Ummati Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* utasema kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametuambia sisi kua Mitume walifikisha Ujumbe wao kwa Watu wao.'

Hivyo hayo ndio maana ya maneno ya aya hii yasemayo: 'Na kadhalika tumekujaalieni Kua Ummah wa Kati na kati na Mtakua mashuhuda kwa Watu na Mtume atakua Shuhuda kwenu.' *(Sunnan Ibn Majah)*

Kwani Ummah wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* umejaaliwa kua Ummah Wasatan kwa sababu pia ya kua yeye mwenyewe ni meenye kuelezewa kama:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا رَحۡمَةٗ لِّلۡعَٰلَمِينَ﴾

Wama Arsalnaka Illa Rahmatan Lil Aalamiina. *(Surat Al Anbiyah 21:107)*

Tafsir: ***Hatukukutuma wewe Isipokua kwa ajili ya kua ni Rehma kwa Walimwengu***

Hivyo basi Uislam ni Rehma, na kila Chenye Rehma hua hakina Misimamo mikali wala Misimamo regevu bali hua kinasimamia Maslahi ya wahusika kwa Ujumla na kwa uadilifu, kama vile ambavyo tutakavyoona namna inavyotakiwa kiwe kusimamo cha I'tidal baina ya Rukuu na Sujud ndani ya Sala.

Na Kitendo cha kuinuka kutoka katika Rukuu na kusimama hadi mgongo ukakaa sawa na kutulia kabla ya kuingia katika hatua ya Kusujudu hua kinajulikana kama I'tidal.Yaani kubakia kwa mda kati kati baina ya hatua mbili kubwa za Sala ambazo ni Rukuu na Sujud.

Kwani anasema Rifai Ibn Rafi *Radhi Allahu Anhu* kua:

كُنَّا يَوْمًا نُصَلِّي وَرَاءَ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، فَلَمَّا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرَّكْعَةِ قَالَ: سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ "، قَالَ رَجُلٌ وَرَاءَهُ: رَبَّنَا وَلَكَ الحَمْدُ حَمْدًا كَثِيرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيهِ، فَلَمَّا انْصَرَفَ، قَالَ: مَنِ المتَكَلِّمُ، قَالَ: أَنَا، قَالَ: رَأَيْتُ بِضْعَةً وَثَلاَثِينَ مَلَكًا يَبْتَدِرُونَهَا أَيُّهُمْ يَكْتُبُهَا أَوَّلُ

‘Sisi tulikua tulikua tukisali Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na alikua anaponyanyua Kichwa chake kutoka kwenye Rukuu basi husema:

سَمِعَ اللهُ لِمَنْ حَمِدَهُ

***Sami Allahu Liman Hamidah yaani Allah* Humsikia Yule anaemsifu**

Na Mtu aliekua Nyuma ya *Rasul ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema:

رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ، حَمْدًا كَثِيْرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيْهِ

***Rabbana wa Laka Alhamd Hamdan Kathiran Tayyiban Mubarrakan Fihi* - Mola wetu Sifa zote ni zako, Sifa Nyingi Sana zilizo Safi na zenye Baraka.**

Hivyo baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumaliza kusalisha basi akauliza: ‘Jee ni nani aliesema:*Rabbana wa Laka Alhamd Hamdan Kathiran Tayyiban Mubarrakan Fihi?’*

Ambapo mtu aliesema akasema: ‘Ni mimi hapa ya *Rasul Allah’*

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Hakika mimi nimeona Malaika Thelathini wakishindana ili kila mmoja miongoni mwao awe ni wa Kwanza kuyaandika maneno hayo.’(*Sahih Bukhari)*

Ambapo kwanza Hadith hii ni yenye kututhibitishia hatua ya I'tidal katika Sala na nini kinaruhusika Kufanywa au kutamkwa ndani yake.

Na pili hadith hii inatuthibitishia kua Kuna mambo ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam hakuyafanya, na wala hakuyaanzisha yeye, lakini hata hivyo Masahaba zake waliyafanya na pia walikua ndio walioyaanzisha, lakini hata hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuyakataza wala kuyapinga kwa kusema kua kwa kua hili sikulianzisha mimi basi ni Bidaa ama ni Haramu.

Na hapa tunazungumzia Ibada ya Sala ambayo *Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* alifundishwa na Mwalimu bora namna ya kuitekeleza Ibada hio ambae ni Malaika Jibril, hivyo kama kila kitu kizuri ambacho hakukifanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kinakua Bidaa na Haram basi bila ya shaka *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angeanza kwanza na maneno haya*:*

رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ، حَمْدًا كَثِيْرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيْهِ

Aliyoyaongeza Sahaba wake Huyu kwenye Ibada ya Sala kama inavyosema Hadith yetu hii.Lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakufanya hivyo kwa sababu Hili Jambo lilikua ni Jema kiasi ya kua hadi Malaika walikua wanapiganiana nani atakua wa mwanzo kuliandika.Na ndio maana Imam Muhammad Idris Al Shafii akasema kua kuna Bidaa nzuri na Bida isiyofaa**.**

Na amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* katika kuelezea namna *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyokua akisali kama isemavyo hadith ifuatayo:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ نُمَيْرٍ، حَدَّثَنَا أَبُو خَالِدٍ، - يَعْنِي الأَحْمَرَ - عَنْ حُسَيْنٍ الْمُعَلِّمِ، ح قَالَ وَحَدَّثَنَا إِسْحَاقُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، - وَاللَّفْظُ لَهُ - قَالَ أَخْبَرَنَا عِيسَى بْنُ يُونُسَ، حَدَّثَنَا حُسَيْنٌ الْمُعَلِّمُ، عَنْ بُدَيْلِ بْنِ مَيْسَرَةَ، عَنْ أَبِي الْجَوْزَاءِ، عَنْ عَائِشَةَ، قَالَتْ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَسْتَفْتِحُ وَكَانَ إِذَا رَكَعَ لَمْ يُشْخِصْ رَأْسَهُ وَلَمْ يُصَوِّبْهُ { الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ }الصَّلاَةَ بِالتَّكْبِيرِ وَالْقِرَاءَةَ بِ وَلِكَنْ بَيْنَ ذَلِكَ وَكَانَ إِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ لَمْ يَسْجُدْ حَتَّى يَسْتَوِيَ قَائِمًا وَكَانَ إِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ السَّجْدَةِ لَمْ يَسْجُدْ حَتَّى يَسْتَوِيَ جَالِسًا وَكَانَ يَقُولُ فِي كُلِّ رَكْعَتَيْنِ التَّحِيَّةَ وَكَانَ يَفْرِشُ رِجْلَهُ الْيُسْرَى وَيَنْصِبُ رِجْلَهُ الْيُمْنَى وَكَانَ يَنْهَى عَنْ عُقْبَةِ الشَّيْطَانِ وَيَنْهَى أَنْ يَفْتَرِشَ الرَّجُلُ ذِرَاعَيْهِ افْتِرَاشَ السَّبُعِ وَكَانَ يَخْتِمُ الصَّلاَةَ بِالتَّسْلِيمِ . وَفِي رِوَايَةِ ابْنِ نُمَيْرٍ عَنْ أَبِي خَالِدٍ وَكَانَ يَنْهَى عَنْ عَقِبِ الشَّيْطَانِ

'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akianza Sala kwa Takbirat na kisomo cha *Alhamd lillahi Rabbi Al Alamiin,* na kisha anaporukuu hua hakiweki Kichwa chake juu wala hakipindishi chini bali alikua akikiweka katikati baina ya Hali mbili hizo. Na kisha anaponyanyua Kichwa Kutoka katika Rukuu basi hua si mwenye Kusjudu Moja kwa moja hadi pale atakaposimama Sawia. Na anaponyanyua kichwa baada ya Kusjudu hua hasjudu tena hadi akae kitako kwanza. Na mwisho wa kila Rakaa mbili hua ni mwenye kusoma At Tahiyyat, na alikua akiulaza kwa kuuweka chini Mguu wake wa Kushoto, na kuunyanyua wa Kulia. Amekataza Kukaa mkao wa Shaytani wa kukalia Visigino (Katika Atahiyyat), na amekataza watu kutanua Mikono yao kama Wanyama wa Mwituni, na alikua akiimaliza Sala yake kwa Kutoa Salam.'(Sahih Muslim)***

Kwani tunapoiangalia Hadithi hii basi ndani yake Imetaja hatua nane za Sala ambazo ni: *Takbirat Al Ihram, Kisomo cha Surat Al Fatiha, Rukuu, Itidal, Sujud, Jalasa (kikao cha baina ya Sijda 2), Tahiyyat* ya kwanza na ya pili na kutoa Salam.

Na kama tulivyoona katika hatua ya I'tidal kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua Akisimama sawia na kuunyoosha mgongo wake, ambapo kama tulivyosema kua hii ni moja kati ya Nguzo za Sala.Kwa maana hio hio basi Inapokosekana I'tidal ndani ya Rakaa husika basi Rakaa hio hua haihesabiki na hivyo Sala husika pia hua haihesabiki kwani inakua ni Batili.

Ingawa kwa Upande wa Imam Abu Hanifa tunaona kua yeye anasema kua: '**Kusimama I'tidal hua kunapendekezwa na wala sio Lazima. Hivyo Mtu akienda moja kwa moja kutoka kwenye Rukuu bila kusimama sawia na akaingia kwenye Sijda basi inaruhusika, na hii ni kwa sababu Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua:**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱرۡكَعُواْ وَٱسۡجُدُواْ وَٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمۡ وَٱفۡعَلُواْ ٱلۡخَيۡرَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Hajj 22:77)*

*Tafsir:**Enyi Wale ambao Mlioamini Rukuuni na Sujuduni Na muabuduni Mola wenu Na Fanyeni Mambo ya KheriIli Mpate kua ni wenye Kufuzu.**(Fat-ul Muin)*

Na ingawa Hadith hii imetaja *Takbirat Al Ihram* tu na haikutaja *Takbirat* nyenginezo lakini hata hivyo Takbirat Nyenginezo zote zenye kuashiria Kutoka kwenye Hatua moja ya Sala kuingia kwenye Hatua nyengine hua niSunna zenye kupendekezwa na hizi hua zinaitwa *Takbrat Al Intiqaal.*

KWANINI HAKUNA TAKBIRAT AL INTIQAL BAADA YA RUKUU

❖❖❖

Neno *Intiqal* hua linamaanisha Kifo, Kuhama kwa kitu kutoka sehemu moja kuelekea katika Sehemu nyengine, Kutoka kwa Kitu katika Hatua moja kuingia katika Hatua nyengine,Kubadilika kwa hali moja na kuingia katika hatua Nyengine kwa kitu. Hali ya Kipindi cha Mpito, hali ya Mabadiliko ya Kitu.n.k.

Hivyo *Takbirat Al Intiqal* ambazo ni tofauti na *Takbirat Al Ihram* hua ni Takbir za Sala zenye kuashiria Kutoka kwenye Hatua moja ya Sala kuingia kwenye Hatua nyengine kutokana na kumalizika kwahio hata husika ambapo*Takbirat Al Intiqaal* za Sala Tano za Kila siku hua ni 94 katika hali ifuatayo:

Katika Salat Al Fajr hua kuna Takbirat Al Intiqaal 11.

Katika Sala Al Maghrib kuna Takbirat Al Intiqaal 17.

Na katika Sala za Rakaa nne zilizobaikia hua mna Takbirat Al Intiqaal 66 ambapo kila Sala ina Takbir Al Intiqaal 22 kwani Sala za Rakaa nne ziko 3 ambazo ni Salat Adh Dhuhr, Salat Al Asr na Salat Al Isha.

Na ingawa*Takbirat Al Intiqal* hutamkwa katika kila mabadiliko ya hatua za Sala lakini hua haitamkwi pale tunapoingia katika Hatua ya kunyanyuka kutoka katika hatua ya Rukuu na kusimama kabla ya

kuingia kwenye hatua ya Kusujudu. Na hii ni kwa sababu amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Salini kama milivyoniona mimi nikisali'** *(Bukhari na Muslim)*

Na akasema tena Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

كانَ رَسولُ اللهِ ﷺ إذا قامَ إلى الصَّلاةِ يُكَبِّرُ حِينَ يَقُومُ، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَرْكَعُ ثُمَّ يقولُ: سَمِعَ اللهُ لِمَن حَمِدَهُ حِينَ يَرْفَعُ صُلْبَهُ مِنَ الرَّكُوعِ ثُمَّ يقولُ: وهو قائِمٌ رَبَّنا ولَكَ الحَمْدُ، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَهْوِي ساجِدًا، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَرْفَعُ رَأْسَهُ، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَسْجُدُ، ثُمَّ يُكَبِّرُ حِينَ يَرْفَعُ رَأْسَهُ، ثُمَّ يَفْعَلُ مِثْلَ ذلكَ في الصَّلاةِ كُلِّها حتّى يَقْضِيَها ويُكَبِّرُ حِينَ يَقُومُ مِنَ المَثْنى بَعْدَ الجُلُوسِ

'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisimama Kusali basi husema *Allahu Akbar,* na kisha anapotaka Kurukuu husema *Allahu Akbar* na kisha husema *Sami Allahu Liman Hamida* na kunyanyuka kutoka kwenye Rukuu na kisha husimama na kusema *Rabbana wa Laka Al Hamd,* Kisha husema *Allahu Akbar* na kuingia kwenye Sijda na kisha hunyanyua kichwa chake na Kusema *Allahu Akbar* na kisha Husema *Allahu Akbar* na Kusujudu tena kisha husema *Allahu Akbar* na kunyanyua Kichwa chake. Na hufanya hivyo katika Sala nzima hadi atakapomalkza Kusali na husema *Allahu Akbar* anaposimama baada ya Kukaa kutoka kwenye Rakaa ya pili.'***(Sahih Muslim)***

Ambapo tunapoiangaliaHadith hii basi tunaona kua inatuonesha Hatua za Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*zilivyokua, yaani alikua baada ya kuingia kwenye Sala kwa kutumia *Takbirat Al Ihram* yaani *Takbira* ya Kuingia ndani ya Sala basi alikua akitumia *Takbirat Al Intiqaal* katika hatua anayobadilisha au anayoimaliza ndani ya Sala husika kabla ya kuingia katika hatua nyengine na hivyo kuashiria kuhama kutoka kwenye Hatua hio na kuingia kwenye Hatua nyengine, isipokua pale anapotoka kwenye Rukuu ambapo hua hatumii *Takbirat Al Intiqaal* bali husema *Sami Allahu Liman Hamidah.*

Ambapo anasema Imam Al Bujaraimi kua:

وَالسَّبَبُ فِي سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ أَنَّ الصِّدِّيقَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ مَا فَاتَتْهُ صَلَاةٌ خَلْفَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَطُّ، فَجَاءَ يَوْمًا وَقْتَ صَلَاةِ الْعَصْرِ فَظَنَّ أَنَّهَا فَاتَتْهُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَاغْتَمَّ بِذَلِكَ وَهَرْوَلَ وَدَخَلَ الْمَسْجِدَ، فَوَجَدَهُ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مُكَبِّرًا فِي الرُّكُوعِ فَقَالَ: الْحَمْدُ لِلَّهِ وَكَبَّرَ خَلْفَهُ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَنَزَلَ جِبْرِيلُ وَالنَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي الرُّكُوعِ فَقَالَ: يَا مُحَمَّدُ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ فَقُلْ: سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ . وَفِي رِوَايَةٍ اجْعَلُوهَا فِي صَلَاتِكُمْ . فَقَالَهَا عِنْدَ الرَّفْعِ مِنْ الرُّكُوعِ، وَكَانَ قَبْلَ ذَلِكَ يَرْكَعُ بِالتَّكْبِيرِ وَيَرْفَعُ بِهِ فَصَارَتْ سُنَّةً مِنْ ذَلِكَ الْوَقْتِ بِبَرَكَةِ الصِّدِّيقِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ

‘Na sababu kuhusiana kutumika *Samia Allahu Liman Hamida* ni kutokana na Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu,* ambae kamwe hakuwahi kutosali nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* hivyo siku moja wakati alipokua anataka kusali Salat Al Asr, basi akachelewa na hivyo akadhania kua hatowahi Rakaa na Kusali nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hivyo akakimbilia Msikitini haraka Sana, na akamkuta *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa katika *Takbirat Al Intiqaal* na kuingia kwenye Rukuu, Hivyo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akasema *Alhamd lillah!* Na kisha Akaingia kwenye Sala kwa Takbir nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na mara akashuka Malaika Jibril na kumkuta *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa bado yupo kwenye Rukuu na hivyo Malaika Jibril akasema : ‘Ewe Muhammad (*Salallahu Alayhi wa Salam*) Allah anawasikia Wanaomtukuza’ hivyo sema *Sami Allahu Liman Hamida.*

Na katika Riwaya nyengine basi inasema kua Malaika Jibril akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Ijaalie *Samia Allahu Liman Hamida* kua katika Sala yako’ Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaitumia katika wakatialipokua akinyanyuka kutoka kwenye Rukuu. Kwani kabla ya hapo basi *Takbirat Al Intiqaal* ndio iliyokua ikitumika katika Kunyanyuka kutoka kwenye Rukuu, hivyo imekua ni Sunnah kuyasema kutokana na Baraka za Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu’*.(*Hashiyyah Bujairimi ala Al Khathi*.)

Riwayah hii pia imenukuliwa kwenye vitabu vya ***Al Miah as-Saniah Min Wasoya Rasulullah Salallahu Alayhi wa Salam*** cha Imam Taha Abdullah Al Afifi***, Hashiyyah Jamal Ala Sharh Manhaj,***cha Imam Sulaiman Al Jamal na pia katika ***Ha Shiyah I'anah Thalibin,*** cha Imam Abu Bakar Muhammad Shatha ad-Dimyati.

Na kwa kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

كُلُّ أُمَّتِي يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ أَبَى قَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ وَمَنْ يَأْبَى قَالَ مَنْ أَطَاعَنِي دَخَلَ الْجَنَّةَ وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ أَبَى

Ummah wangu wote utaingia Peponi isipokua wale watakaokataa, Hivyo Masahaba wakasema: ‘Ya Rasul Allah na jee ni nani hao watakaokataa?’ *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Yeyote yule atakaenitii mimi basi atainga Peponi, atakaekataa kunitii mimi hua ni mwenye kukataa kuingia Peponi’*(*Sahih Bukhari)*

Basi kwetu sisi hua ni Wajib kutekeleza Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayh wa Sala*m ili tusije tukawa nimiongoni mwa waliokataa.

Na anasema Imam An Nawawi kua: ‘***Takbirat Al Intiqal* hua ni Sunnah, na hivyo kama ikiwa haikutamkwa basi Sala hua haibatiliki ila hukosekana Malipo na fadhila *zaTakbiratAl Intiqal* ndani ya Sala husika.’** *(Al Minhaj fi Sharh Sahih Muslim)*

Na amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema Allahu Akbar kila anapoinama na kuinuka na anaposimama na kukaa, na ndivyo pia alivyokua akifanya Abu Bakr na Umar *Radhi Allan Anhum*.’***(*Imam Tirmdhii)*

Hivyo Wanazuoni wanakubaliana kua *Taqibrat Al Intiqal* ni Sunna, isipokua kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Is-haq Ibn Rahawayh kwani wao wanasema kua ni Wajib. *(Mawsuah Al Fiqhiyyah Al Kuwaytiyah)*

Na amesema Imam Imran Al Yamani kuhusiana na Takbirat Al Intiqal ya Kusjudu kua: 'N**i Sunna kuanza *Takbir Al Intiqal* pale unapotaka kuenda chini kusujudu na kuimalizia pale unaposujudu, na hii ni kwa sababu Sujud hua ni Kitendo cha Ndani ya Sala hivyo ni Sunna Kuivuta Takbir ili isije ikawa imejitenganisha na Dhikr na kufanana na vitendo vyengine vya Sala.'***(Al Bayan Fi Madhhab Imam Al Shafii)*

Na Shaykh ul Islami Mujtahid Imam Shams Ad Din Al Rafii basi yeye anasema kua: '***Takbirat Al Intiqal ya* kunyanyuka kutoka katika Sijda na kusimama hutamkwa baada ya kutoka kwenye Sijda na kukaa na kisha unaponyanyuka unaitamka moja kwa moja hadi utakaposimama'** *(Al Talkhis Al Khabir)*

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi inapendekezwa Kuivuta *Allaaahu Akbar* hadi herufi Lam kua katika mvuto wa Harkah Saba ili *Takbirat Al Intiqal* iwe ndefu.

Ambapoanasema Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua:**'Miongoni mwa wenye Mtizamo wa kua Takbirat Al Intqal ni Sunnah ni pamoja na Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu,* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu,* Qais Ibn Ubaydah *Radhi Allahu Anhu,*Imam Ash Shaabi, Imam Al Awzai, Imam Said Ibn Abd Al Aziz, Imam Abu Hanifa, Imam Malik Ibn Anas na Imam Muhammad Idris Al Shafii.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Al Hasan Ali Ibn Khalaf Ibn Abd Al Malik Ibn Battal basi yeye anasema kua: **'Miongoni mwa wenye Mtizamo wa kua *Takbirat Al Intiqal* ni Sunna ni pamoja na Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu,* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Abd Alah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu,* Abu Hurayra *Radhi Allahu Anhu,* Imam Makhul, Imam Ibrahim An Nakhai na Imam Abu Thawr.'**

Kwani Hikma na Busara ya Kutumika *Takbirat Al Intiqal* katika Kila hatua ya kituo cha Sala, mbali ya kua ni kutofautisha sehemu hatua hizo, lakini pia matumizi ya Maneno *Sami Allahu Liman Hamida* baada ya Rukuu badala ya Takbirat Al Ihram hua ni kwa ajili ya kumtofautishia Maamuma asiemuona Imam, Vipofu ili waweze kujua kua hio ilikua ni Rukuu na hivyo Imam anatoka kwenye Rukuu na Kusimama kwa ajili ya kujitaharisha kuingia katika Sijda. **Na ndio maana kila *Takbirat Al Intiqal* na Kila Tasmih - *Sami Allahu Liman Hamida* -hua inatakiwa iende Sambamba na kitendo husika kinachowakilishwa kutokana nayo.**

Na anasema Imam An Nawawi juu ya hili kua: '***Takbirat Al Intiqal* ya Kurukuu inatakiwa Itamkwe sambamba na kitendo cha Kurukuu, na Takbira ya Kusujudu sambamba na kitendo cha kuelekea chini katika Kusujudu, Takbirat ya Kusimama kutoka kwenye Sujudu itamkwe katika wakati wa Kunyanyuka n.**k'*(Sharh Muslim)*

Imam An Nawawi anaendelea kutuambia kua: '**Kwa Imam hua ni Wajib kutamka *Takbirat Al Intiqal* kwa Sauti, na kwa Maamuma na wanaosali peke yao pia hua wanatakiwa Watamke kwa Kimya Kimya'***(Al Majmuu)*

Ambapo kwa upande wa Imam Ali Shurunbulali Al Hanafi basi yeye anasema kua: **'Hua ni Sunna kwa Imam kupaza Sauti katika Kutamka Takbir na kisha kusikiliza, kwa ajili ya kuwajuulisha**

Maamuma wake mwanzo wa Sala na mabadiliko hatua za Sala Na Maamuma na anaesali peke yake hua hatakiwi kupaza sauti anapotamka Takbir zake.*(Maraqi Al Falah)*

Ama kwa upande wa Imam Al Muhaqqiqin Shaykh Ul Islami Imam Ibn Hajar Al Haythami basi yeye anasema kua: **'Hua ni Sunna kwa Imam kuoaza Sauti kubainisha *Takbirat Al Ihram na Takbiral Al Intiqal,* na kwa Maamuma kutamka kimya kimya, ambapo ndani yake Takbira hizo muwe na nia ya kua hio ni *Dhikr Allah* na wala si venginevyo kwani ikiwa vyenginevyo basi Sala itabatilika'*(Tuhfa Al Muhtaj)*

Na hii ni kwa sababu Amesema Muawwiyah Ibn Al Hakam *Radhi Allahu Anhu* kua:'**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kwa Hakika Sala kamwe haiwezekani kuambatanishwa na Maneno ya Mazungumzo, kwani kinachostaihiki ndani ya Sala hua ni Tasbih Takbir, na Kisomo cha Qur'an'***(Sahih Muslim, Sunnan Abu Daud)*

Ambapo Al Imam Al Khatib Al Shirbini anasema kua: '**Hoja inakuja katika Kupaza sauti kwa ajili ya Takbir au kwa Ajili ya Kuisikiliza Takbir? Hivyo kama ikiwa nia ni Kutamka Takbir au Kusikiliza Takbir kutoka Kwa Maamuma baada ya Kuwajuulisha kinachofuatia, basi Sala hua haibatiliki lakini kama ikiwa ni vyenginevyo basi inabatilika'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Na Imam Zain Ad Din Al Malibari akasema pia kua: '**Kisharia hua inatakiwa kupaza Sauti kwa Takbirat Al Intiqal na Taqbirat Al Ihram kwa Imam, na kwa Maamuma pia kama itahitajika kufanya hivyoLakini iwe ni Lazima kwa nia ya kua ni dhikkr Allah au kuisikiliza, kwani ikiwa vyenginevyo basi Sala husika hubatilika kama walivyosema Maimam wetu katika Al Minhaj'***(Fat-h Al Muin)*

Hivyo *Takbir Al Ihram, Takbirat Al Intiqal na Tasmih (Sami Allahu Liman Hamida)* zinatumika ndani ya Sala kwa ajili ya Kumrahisishia Imam na Maamuma katika Jumuiko moja la Sala husika na tofauti za hatua zake ndani yake

Na kuhusiana na *Takbir Al Intiqalat* na *Tasmih* baina ya Hatu za Sala hua ni Dhikr Allah, lakini kama ikitamkwa kwa nia ya Kuisikiliza utamu wake kama Dhikr Allah basi hua ni bora zaid, kwani ndivyo inavyotakiwa Kuonja Ladha ya Utamu wa Ibada ya Sala

Kwani anasema Imam Ali Muhammad Ibn Habib Al Mardawi Al Hanbali kua: '**Kama ikiwa Mtu ataitamka *Takbir Al Intiqal* ya Kuenda chini na kuja Juu katika Sala katika Wakati anatekeleza Vitendo hivyo na kisha akaimalizia Takbira hio kabla ya Kumalizika vitendo hivyo, basi Takbir hio hua haitoshelezi, kwa Sababu hua imetekelezwa sivyo, nahakuna kutofautiana kwa Wanazuoni Juu ya Jambo hilo,**

Na pia kama Mtu akianza kuitamka kabla ya kuanza kitendo husika cha Sala, au akaitamka mpaka baada ya kumalizika kitendo cha Sala, basi hua ni sawa na Mtu ambae hakuitekeleza Takbir hio, na hii ni kwa Sababu ameitekeleza nje ya mipaka yake, yaani mtu huyo hua ni sawa na Anaemalizia kisomo cha Quran katika wakati wa Kurukuu, au anaeanza kusoma Attahiyat kabla ya kukaa kitako.' *(Al Insaaf)*

Na Ingawa huenda mtu huyo akasamehewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kosa hilo, lakini katika hali kama hii basi inakua ni vigumu kutoa Hukmu na kusema kua jambo hili kinaweza kumbatilishia Sala yake au labda kusema kua itambidi atekeleze Sijda sahw.

Kwani ingawa hapa panazungumziwa *Takbir Al Intiqal* lakini ndani yake pia mnajumuishwa na *Tasmi* yaani Kusema *Sami Allahu Liman Hamida*, kwani hukmu ya *Takbirat Al Intiqal na* Tasmi hua zote ni sawa kwanini miongoni mwa Dhikr Allah zenye kudhihirisha mipaka ya hatua katika hatua za Sala.

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii basi hua ni Sunna kutimiza Adabu za Kurukuu na Kunyanyuka kutoka kwenye Rukuu ya Sala kwa kusema *Allahu Akbar* huku ukinyanyua Mikono yako yote miwili hadi Mabegani kama ifanywavyo katika *Takbirat Al Ihram* kwenye kama tulivyoelezea katika sehemu ya *Rafa al Yadayn.*

Na pia kunyanyua mikono unapotoka kwenye Rukuu huku ukiwa ni mwenye kusema *Sami AllahuLiman Hamida* na kisha unaposimama sawia huku mikono yako ikiwa umeiachia pembeni mwako yaani bila ya kuifunga.Na kisha hapa katika hatua hii sasa ndio unasoma Dua inyojulikana kama Duaa Al Qawma ambayo ni:

ربنا ولك الحمد

‘***Rabbana Wa Laka Al Hamd’***

Na Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Duaa al Qawma pale inapokua Sala inayosaliwa ni Sala ya Jamaa.

Kwani anasema Imam An Nawawi kua: ‘**Al Shafii amesema kua Inapendekezwa kufanya Adhkar hizi kwa Imam, kwa Maamuma na kwa Mtu anesali Peke yake kusema, yaani Kila mtu anatakiwa atamke zote *Sami Allahu Liman Hamida na Rabbana Laka Al Hamd.’*** *(Al Majmuu)*

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: ‘**Na hakuna kutokukubaliana juu ya Hili katika Madhhab yetu. Na hii inathibitishwa na Hadith iliyomo katika Sahih Bukhari ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi w Salam* amesema kua: ‘Salini kama mlivyoniona miminilivyokua nikisali’ hivyo hadith hii inatilia mkazo umuhimu wa kila Mtu anaesali, kua ni mwenye kutakiwa kuchanganya *Dhikr Allah* mbili hizo katika kuzitamka, na hii ni kwa sababu kama ilivyosemwa katika hadithi nyengine pia Kile kilichopendekezwa kwa Imam kukifanya basi kimependekezwa kwa Maamuma pia katika Sala zao kama Tasbih katika wakati wa Kurukuu. nk** *(Al Majmuu)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anasema katika sehemu nyengine kua**: ‘Kulingana na Mtizamo wa Kauli inayotegemewa hua Madhhab ya Imam Al Shafii, basi ni kua:** ‘**Hua ni Sunna kwa Imam na Maamuma na kila anaesali peke yake**. **Kua ni mwenye Kusema Sami *Allahu Liman Hamida* pale anaponyanyuka kutoka Kwenye Rukuu na pia kusema *Rabbana Wa Laka AlHamd* pale anaposimama sawia katika *Al Itida***l.*’*(*Rawdha Al Talibin)*

Na hii ni kutokana na Uthibitisho wa ile Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua**:**

كَانَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم إِذَا قَالَ: سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ. قَالَ : اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ

‘**Alikua Nabii *Salallahu Alayhi wa Salam*anaposema*Sami Allahu Liman Hamida*husema *AllahumaRabbana wa Laka Al Hamd’*** (*Sahih Bukhari)*

Ambapo Mtizamo huu wa Madhhab ya Imam Al Shafii ndio pia Mtizamo wa Imam Ata Ibn Abi Rabah, Imam Muhammad Ibn Sirin, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Burdah n.k. *(Nihayat Al Muhtaj)*

Ama tunapozungumzia kuhusiana na Sala ya Mtu peke yake basi anasema Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki na Imam Abu Jafar Al Tahawi kua: '**Wanazuoni wanakubaliana kua Mtu anapokua anasali peke yake basi asome *Tasmih (Sami Allahu liman Hamida)* anaponyanyuka kutoka kwenye Rukuu Na pia asome At *Tahmid (Rabbana wa Laka Al Hamd)* pale anapokua tayari ameshasimama sawia, kwani juu ya hili kua Ijmaa (Makubaliano ya Wanazuon**i.'*(Sharh Maani Al Athar/Al Istidhkar*)

Hapa tunarudi kwa Imam wa Maimam na Watoto wa Maimam waliokua pia Maimam, huyu ni Imam maarufu wa Madhhab ya Imam Al Shafii alieishi kwa Mda wa Umri wa miaka 103 ambapo aliwasomesha pia na Wajukuu wa Wanafunzi wake, Jee tunamjua Imam Gani huyo?

Huyu si Imam mwengine yeyote bali ni Shaykh Ul Islami Al Faqih Imam Abu Yahya Zayn Ad Din Zakarriyah Al Ansari Al Shafii, ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake unakunata na kina Mujtahid Imam Al Bulqini, Imam Al Qastallani, Imam Al Sakhawi Imam Al Suyuti, Imam Al Sharani, Imam Shihab Ad Din Al Raml, na mtoto wake ambae ni Imam Shams Ad Din Al Ramli, Al Muhaqqiq Imam Ibn Hajar Al Haythami, Imam Al Khatib Al Shirbin, n.k

Hivyo anasema Imam Zakarriyah Al Ansari Al Shafii kua: '**Kusoma *Tasmi(Sami Allahu Liman Hamida*) ni kwenye kufahamika kwa Masahaba, kutokana na Hadith iliyosema kua:**

فَإِنَّهُ مَنْ وَافَقَ قَوْلُهُ قَوْلَ الْمَلاَئِكَةِ غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ

Kama Kauli ya mmoja wenu ikienda Sambamba na Kauli ya Malaika basi Dhambi zote za mtu huyo zilizopita zitasamehewa,*(Imam At Tirmidhi)*

Ambapo maana ya Hadith hii ni kua Imam atakaposema *Tasmi* basi na nyinyi someni *Tasmi* kama mnavyojua na pia *Tahmid*Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaambia Masahaba zake wasome *Tahmid* kwa sababu yeye alikua akisoma kimya kimya hivyo wao walikua wakiisikia *Tasmi* yake tu ambayo ilikua ni ya Sauti.'*(Asna Matalib)*

Kwani amesema Hudhayfah Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema pale anaponyanyuka kutoka kwenye Rukuu:*Sami Allahu Liman Hamida, Rabbana wa Laka Al Hamd.'****(Sahih Muslim)*

Na amesema pia Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*katika hadith ifuatayo kua:

حَدَّثَنَا مَحْمُودُ بْنُ غَيْلاَنَ، حَدَّثَنَا أَبُو دَاوُدَ الطَّيَالِسِيُّ، حَدَّثَنَا عَبْدُ الْعَزِيزِ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي سَلَمَةَ الْمَاجِشُونُ، حَدَّثَنِي عَمِّي، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ الأَعْرَجِ، عَنْ عُبَيْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي رَافِعٍ، عَنْ عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِبٍ، قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم إِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ قَالَ " سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ مِلْءَ السَّمَوَاتِ وَمِلْءَ الأَرْضِ وَمِلْءَ مَا بَيْنَهُمَا وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ "

Amesema Muhammad Ibn Ghaylani, kua amesema Abu Daud ambae ni At Tayalisi kua amesema Abd Al Azizi Ibn Abd Allah Ibn Abi Salama Al Majishun kua amesema Aamii kua amesema Abd Rahman Al Araji kua amesema Abd Allahi Ibn Abi Rafii kua amesema Ali In Abi Talib kua *Rasul*

Allah Salallahu Alayhi wa Salam **alikua akisema anaponyanyua Kichwa chake kutoka kwenye Rukuu kua:**‘***Rabban Laka Al Hamdu Mila as Samawati wa Al Ardhi wa Mila a Mashi ita min Shay-in Baadu (Ewe Mola wetu Shukran zote ni zako, Zinazojaa Mbinguni, na Ardhini*** **na kila sehemu Unayotaka kujaza)’’***(Imam At Tirmidhii, Sahih Muslim,Musnad Imam At Tayalisi,At Tahqiq Ibn Jawzi, Imam Al Bayhaqi na Sunnan Abu Daud)*

Ambapo maneno ya hadithi hii tena yamenukuliwa kutoka kwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, na Ibn Abi Awfa *Radhi Allahu Anhu,* na Abi Juhayfa na Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu.*

Na amesema amesema Imam Abu Isa Al Tirmidhii kuhusiana na Hadith hii kua : ‘**Hadith hii ya Ali ni Hadith Hasan Sahih.’**

Abu Said Al Khudri, *Radhi Allahu Anhu,* amesema pia kua: **‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alipokua akinyanyua kichwa chake kutoka kwenye Rukuu basi alikua akisema:**

رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ

مِلْءَ السَّمَاوَاتِ وَمِلْءَ ٱلْأَرْضِ وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ. أَهْلَ الثَّنَاءِ وَالْمَجْدِ، أَحَقُّ مَا قَالَ الْعَبْدُ، وَكُلُّنَا لَكَ عَبْدٌ. اَللَّهُمَّ لاَ مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ، وَلاَ مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ، وَلاَ يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ

RAbbanaa lakal hamdu mil assamaawaati wa mil al ardhi wa mil a maa shi’ta min shai in ba’du ahlutstsanaa i walmajdi a haqqu maa qoolal ‘abdu wa kullunaa laka ‘abdan, Allaahumma laa maa ni’a limaa a’toyta wa laa mu’tiya limaa mana’ta wa laa yanfa’u dhaal jaddi minkal jaddu

Ewe Mola wetu Shukran zote ni zako, Zinazojaa Mbinguni, na Ardhini **na kila sehemu Unayotaka kujaza,** ***Wewe ni mwenye kustahiki Utuku wa Sifa zote, mwenye kustahiki Anayosema Mja, na kila mmoja miongoni mwetu ni mja wako, Ya Allah hakuna anaeweza kuzuia unachotoa na anaeweza kutoakile unachokizuia Utajiri hua haumnufaishi Mtu Tajiri bila ya kutaka kwako’****(Sahih Muslim)*

Na amesema Imam Ad Daraqutni kua: ‘**Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Imam anaposema: *Sami Allahu Liman Hamida* basi na waliokua Nyuma yake nao waseme *Sami Allahu Liman Hamidapia.’***

Na ukweli ni kua wengi sana miongoni mwa Waislam katika Jamii yetu wanaposali Jamaa basi Imam anaposema *Tasmi - Sami Allahu Liman Hamida,* basi wao hua si wenye kuitamka Tasmi bali hua ni wenye huitikia tu kwa *Tahmid - Rabbana wa Laka Alhamd*, jambo ambalo kwa upande wa Madhhab ya Imam A Shafii hua si Sahih.

Ambapo kwa upande wa Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Naqib Al Misri basi yeye anasema kua**: ‘Njia Bora Unapotoka kwenye Rukuu hua ni kunyanyua mikono na kichwa pamoja huku ukisema *Sami Allahu Liman Hamida*hii inatakiwa kusemwa na kila mtu iwe Imam, Maamuma, au anaesali peke yake**. **Na kisha unaposimama sawia basi unatakiwa kusema *Rabban Laka Al Hamdu Mila as Samawati wa Al Ardhi wa Mila a Mashi ita min Shay-in Baadu(*Ewe Mola**

wetu Shukran zote ni zako, Zinazojaa Mbinguni, na Ardhini na kila sehemu Unayotaka kujaza)'*(Umdat Salik)*

Hivyo Kufanya: ***Tasmi -Sami Allahu Liman Hamida na Tahmid- Rabbana Laka Al Hamd*** hua ni Awla Zaid!

Ambapo kwa upande wa Madhhab mengine yote basi wengi miongoni mwa Wanazuoni wao ni wenye kusema kua: **Katika Sala ya Jamaa wakati Imam anaposema *Sami Allahu Liman Hamida,* basi Maamuma hatakiwi na yeye Kurudia Maneno hayo bali anatakiwa kusema *Rabbana wa Laka Al Hamd* t**u*(Al Hawi Al Fatawi)*

Na amesema **Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

إِنَّمَا جُعِلَ الإِمَامُ لِيُؤْتَمَّ بِهِ فَإِذَا كَبَّرَ فَكَبِّرُوا وَإِذَا رَكَعَ فَارْكَعُوا وَإِذَا قَالَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ . فَقُولُوا اللَّهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ

Imam amejaaliwa kua ni mwenye kufuatwa hivyo anaposema Allahu Akbar, basi nanyi semeni Allahu Akbar, na Rukuuni pale anaporukuu na anaposema: *Sami Allahu Liman Hamida* basi semeni*Rabbana Laka Al Hamd.'**(Sahih Muslim)***

Ambapo kuhusiana na tofauti ya Mitizamo zaidi juu ya ***Tasmi -Sami Allahu Liman Hamida na Tahmid - Rabbana Laka Al Hamd*** basi anasema Imam Ash Shawqani katika Nayl Al Awtar kua**: 'Imam Al Awzai, Imam Sufyan Ath Thawry na kunariwaya moja kutoka kwa Imam Malik ambao wanasema kua: 'Ni Imam na anaesali peke yake tu ndio wanaotakiwa kusema Tasmi na Tahmid, ambapo anaemfuata Imam au Maamuma basi yeye anatakiwa kusema *Rabbana wa Laka Alhamd tu''***

Na Imam Abu Hanifa anasema kua: **'Imam na anaesali peke yake basi wote wanatakiwa kusema Tasmi na Tahmid na anaemfuta Imam anatakiwa aseme *Rabbana wa Laka Al hamd* tu.'**

Ambapo mtizamo huu wa Imam Abu Hanifa ndio pia mtizamo wa Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri, ambae yeye pia amesema kua Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Lakini Imam Abu Yusuf na Imam Muhamamd Ash Shaybani ambao ni Wanafunzi wa Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: 'Imam na Mtu anaesali peke yake basi wote wanatakiwa kutamka Tasmi na Tahmid, na Yule anaemfuata Imam basi anatakiwa aseme *Sami Allahu Liman Hamida* tu.'*(Nayl Al Awtar)*

MASHARTI YA ITIDAL AL QAWMA

❖❖❖

Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Itidal hua ina Masharti yafuatayo:

1-Haitakiwi kua na Lengo lolote lile isipokua Lengo la kua ni Sehemu ya Ibada ya Sala.

2-Inatakiwa Kusimama kwa Mda Mfupi tu.

3-Kisimamo kinatakiwa kisizidi Mda wa zaidi ya kusoma Surat Al Fatiha, na hii ni kwa sababu Itidal ni nguzo fupi ya Sala na hivyo haitakiwi kurefushwa.

Na ingawa hayo ndio Masharti makuu ya *Itidal* lakini hata hivyo, kuna baadhi ya Nyakati au baadhi ya hali hua zinapelekea Itidal kuhitajika Kurefushwa na hua inaruhusika pale inapotokea hali kama hizo.Kwa mfano tuseme Katika Nyakati ambazo Mtu inabidi usome Dua ya Qunut Ndani ya Sala kama Sala ya Al Fajir na Salat Al Witri, ambapo kuhusiana na Qunut zake na Uthibitisho wake kulingana na Hadith na Mitizamo ya Wanazuoni basi tutazungumzia baadae, In-shaa Allah.

Kwani anasema **Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din** Imam Abu Zakarriyah Yahyah Ibn Sharraf An Nawawi kua: '**Mtizamo Mkuu wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni kua Kurefusha Nguzo Fupi ya Sala hua ni Moja kati ya mambo yanayobatilisha Sala**. **Ambapo Miongoni mwa Nguzo fupi basi hua ni Itidal yaani Kisimamo kinachofuatia baada ya Rukuu na kabla ya Sujud**. **Hivyo inatakiwa kaa Mtu mwenye Kusali asiirefushe Itidal baada ya Kurukuu kwake kwa hadi kufikia zaidi ya urefu wa Kisomo cha Surat Al Fatiha**. **Na hii ni kwa sababu Itidal ni Nguzo fupi hivyo hairuhusiwi kuirefusha isipokua kwa Sala ya Qunuti na Tasbih'***(Al Mutammad fii Al Fiqh Al Shafii)*

Ambapo tunapoangalia katika kitabu cha *Al Majmuu* basi tunaona kua Imam An Nawawi anasema pia kua: '**Na Wanazuoni wa Khurasan (Wa Madhhab ya Imam Al Shafii) basi wanasema kua Itidal ya kutoka kwenye Rukuu ni Nguzo Fupi**. **Na kwa kua ni Nguzo fupi basi hua inatakiwa Iwe Nyepesi (Isiyochukua Mda mrefu)**. **Hivyo kama ikiwa itarefushwa kwa Makusudi kama kwa Mtu kukaa kimya ndani yake kaa mda mrefu, Kusoma Dua isiyohitajika Ndani yake, au kwa Dhikr nyenginezo zisizokua na uthibitisho basi hua haikubaliki na huu ndio Mtizamo Sahih kutoka kwa Imam Al Haramayn na pia kwa Imam Al Baghawi,kua kufanya hivyo kunabatilisha Sala, isipokua kwa mambo yanayokubalika kisharia tu.'** *(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Kwani ingawa kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua moja kati ya masharti ya Al Itidal ni kua inatakiwa iwe Fupi kutokana na kua Itidal (Kisimamo baina ya Rukuu na Sujud) yenyewe ni Nguzo Fupi

Lakini kwa upande mwengine basi kuna Hadith isemayo kua:**'Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu kua:***

مَا صَلَّيْتُ خَلْفَ أَحَدٍ أَوْجَزَ صَلَاةً مِنْ صَلَاةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فِي تَمَامٍ كَانَتْ صَلَاةُ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مُتَقَارِبَةً وَكَانَتْ صَلَاةُ أَبِي بَكْرٍ مُتَقَارِبَةً فَلَمَّا كَانَ عُمَرُ بْنُ الْخَطَّابِ مَدَّ فِي صَلَاةِ الْفَجْرِ وَكَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا قَالَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ قَامَ حَتَّى نَقُولَ قَدْ أَوْهَمَ ثُمَّ يَسْجُدُ وَيَقْعُدُ بَيْنَ السَّجْدَتَيْنِ حَتَّى نَقُولَ قَدْ أَوْهَمَ

Sijapata mimi kuwahi kusali nyuma ya Mtu ambae Sala yake imekamilia zaidi ya Sala ya *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* kwa kiukamilifu.Sala yake Ilikua sawia baina ya Nguzo moja na nyengine. Na Sala ya Abu Bakr ilikaribiana kiurefu baina Nguzo moja na Nyengine. Na Sala ya Umar alipokua akisalisha aliirefusha Sala ya Alfajir.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwahi kusema *Sami Allahu liman Hamida* na kisha akasimama hadi tukasema kua amejisahau, na kisha akasjudu na kukaa baina ya Sijda mbili mpaka tukasema kua amejisahau.*(Sahih Muslim, Sunna Abu Daud).*

Ambapo anasema Imam Muhammad Shams Al Haq Adhim Abadi kua: **'Hadith hii inaonesha kua inaruhusika Kurefusha Itidal na Kikao baina ya Sijda mbili'***(Aun Al Ma'bud Sharh Sunnan Abu Daud)*

Na akasema Imam Al Shawqani kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hadith hi ni Uthibitisho wa kua inaruhusika kurefusha Itdal na pia kikao cha baina ya sijda Mbili, mbali ya kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanasema kua Sala ya Mtu anaerefusha Itidal na Kikao cha bainaya Sijda mbili hua inabatilika kwa sababu ya kua hua inavunja Mfululizo stahiki wa Nguzo za Sala. Na amesema Imam Ibn Daqiq Al Idd kua Hii ni hadith inayoonesha kua Itidal ni miongoni mwa nguzo ndefu za Sala, kwani hadith ya Anas inathibitisha hivyo'***(Nayl Al Awtar)*

Kwani wenye kusimamia Mtizamo huu wanatumia pia Uthibitisho wa Hadith isemayo:**'Amesema Hudhayf Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* kua:**

فَكَانَ رُكُوعُهُ نَحْوًا مِنْ قِيَامِهِ، ثُمَّ قَالَ: سَمِعَ اللهُ لِمَنْ حَمِدَهُ، ثُمَّ قَامَ طَوِيلًا قَرِيبًا مِمَّا رَكَعَ، ثُمَّ سَجَدَ، فَقَالَ: سُبْحَانَ رَبِّيَ الْأَعْلَى، فَكَانَ سُجُودُهُ قَرِيبًا مِنْ قِيَامِهِ

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali na akarukuu ambapo Rukuu yake ilikua ni sawa naKisimamo chake,na kisha akasema *Sami Allahu Liman Hamida* na akasimama katika kisimamo ambacho ni sawa na Rukuu yake. Kisha akasjudu na akasema *Subhana Rabbi Al Aala* ambapo katika Kusjudu kwake kulikua sawa na Kisimamo chake**.*(Sahih Muslim)*

Na tunaporudi kwenye Al Majmuu ya Imam An Nawawi kuhusiana na Hadith ya Anas Ibn *Malik Radhi Allahu Anhu b*asi yeye anaturudisha tena kwenye Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kwa kutuambia kua: '**Hadith hii inatuonesha wazi kua Inaruhusika kurefusha Itidal lakini kwa *Dhikr Allah.****(Al Majmuu)*

Hivyo miongoni mwa mifano ya *Dhikr Allah* zinazoruhusika katika Itidal pamoja na ile ya mfano wa Hadith ya Rifaa Ibn Rafii *Radhi Allahu Anhu* pale aliposema:

كُنَّا يَوْمًا نُصَلِّي وَرَاءَ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، فَلَمَّا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرَّكْعَةِ قَالَ: سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ "، قَالَ رَجُلٌ وَرَاءَهُ: رَبَّنَا وَلَكَ الحَمْدُ حَمْدًا كَثِيرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيهِ، فَلَمَّا انْصَرَفَ، قَالَ: مَنِ المتَكَلِّمُ، قَالَ: أَنَا، قَالَ: رَأَيْتُ بِضْعَةً وَثَلاَثِينَ مَلَكًا يَبْتَدِرُونَهَا أَيُّهُمْ يَكْتُبُهَا أَوَّلُ

'**Tulikua tukisali pamoja na Rasul *Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na alipoinuka kutoka katika Rukuu akasema *Sami AllahuLimam Hamida* na mmoja kati ya Masahaba akasema:**

رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ، حَمْدًا كَثِيْرًا طَيِّبًا مُبَارَكًا فِيْهِ

Rabbana wa Laka Al Hamd Hamdan Kathiran Tayyiban Mubaraka Fiihi. **Na baada ya kusali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza Jee ni nani alkesema maneno hayo?'**

Mtu huyo akasema Ni Mimi Ya *Rasul Allah!*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Nimewaona mimi Malaika zaidi ya 30 wakipiganiana ili kila mmoja awe wa kwanza kuyaandika maneno hay**o.'*(Imam An Nasai)*

Ambapo anasema Imam Ibn Rajab Al Hanbali kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hadith hii inaonesha faida za *Dhikr Allah* hii katika Sala, na pia kua Maamuma anaruhusika Kuongezea Tahmid na Sifa nyengine za Kumtuiiza *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Kama unavyoonyesha Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Kauli moja kutoka kwenye Madhhab ya Imam Hanba, kua mfano mzuri ni kufanya Dhikr katika Itidal kuliko katika Rukuu kwa Sala ya Fardhi na hii ni kwa Sababu Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua wanasali Nyuma *ya Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* katika Sala za Fardhi na si katika Sala za Sunna. Hadith hii pia inatuonesha kua Si Makruh kwa Maamuma kunyanyua sauti kwa mara moja katika wakati anapokua nyuma ya Imam.'***(Fat-h Al Barr li Ibn Rajab)***

Na mfano mwengine pia ile hadith ya Abu Awfa *Radhi Allahu Anhu* isemayo:

كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، إِذَا رَفَعَ ظَهْرَهُ مِنَ الرُّكُوعِ، قَالَ: سَمِعَ اللهُ لِمَنْ حَمِدَهُ، اللهُمَّ رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ، مِلْءُ السَّمَاوَاتِ، وَمِلْءُ الْأَرْضِ وَمِلْءُ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْد

'***Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* aliponyanyuka kutoka katika Rukuu alisema:*Sami Allahu liman Hamida, Allahuma Rabban Laka Al HamduMil ai Samawati wa Mil ai Al Ardhi wa Mil ai Shiita Min shay-in Baadu* - Allah Humsikia anaemsifu, Ewe Allah Mola wetu Mlezi Mwenye Sifa Tukufu zinazojaa Mbinguni na Ardhini na Kila sehemu utakayokuijaza***(Sahih Muslim)**

Na Hadith ya Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* isemayo:

كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ قَالَ : رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ مِلْءُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ، وَمِلْءُ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ، أَهْلَ الثَّنَاءِ وَالْمَجْدِ، أَحَقُّ مَا قَالَ الْعَبْدُ، وَكُلُّنَا لَكَ عَبْدٌ، اللهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا أَعْطَيْتَ، وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ، وَلَا يَنْفَعُ ذَا الْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ

Alikua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliponyanyuka kutoka katika Rukuu basi alisema:*Rabban Laka Al Hamd Mil ai Samawati wa Mil ai Al Ardhi wa Mil ai Shiita Min shay-in Baadu, Ahla Althanai wa Al Majid, Ahaqa Ma Qala Al aAbdu, Allahuma La ManiaAa Lima A'aTayta wala MuA'utiLima Manaatta, wala YanfaAu dha AlJaddi Minka Al Jadd'

Ewe Allah Mola wetu Mlezi Mwenye Sifa Tukufu zinazojaa Mbinguni na Ardhini na Kila sehemu utakayokuijaza, Unastahikiza zaid ya Unavyosifiwa na Mja, na kila Mmoja wetu ni Mja wako, Ya Allah Hakuna Kinachoweza kuzuia kile utoacho, wala hakuna kinachoweza kukitoa kile ukizuiacho Na Juhudi zote hazifai kitu bila Idhini yako kwa Nguvu na uwezo wote ni kutoka kwako'*(Sahih Muslim)*

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hii ni Hadith ambayo ina Manufaa mengi miongoni mwao ni kua hua ni Sunna Kutamka Dhikr hii katika Itidal na pia inaonesha kua hua ni Wajib kwa anaesali kubakia katika hali ya Utulivu anapokua katika Itidal'***(Sharh Sahih Muslim)*

Hivyo hizi ndio Dhikr zinazokubalika kusomwa katika Itidal na bila ya shaka ndani yake pia katika yaliyoruhusika hua ni Dua ya Qunut.

7-SUJUD

❖❖❖❖

﴿ سَبِّحِ ٱسْمَ رَبِّكَ ٱلأَعْلَىٰ﴾

Sabbihi isma rabbika Al aAAla *(Surat Al Aala 87:1)*

Tafsir: **Litukuze Jina la Mola wako Alie Juu zaidi kiutukufu.**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱرْكَعُواْ وَٱسْجُدُواْ وَٱعْبُدُواْ رَبَّكُمْ وَٱفْعَلُواْ ٱلْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Hajj 22:77)*

Tafsir: ***Enyi Wale ambao Mlioamini Rukuuni na Sujuduni Na muabuduni Mola wenu Na Fanyeni Mambo ya Kheri Ili Mpate kua ni wenye Kufuzu***.

Na amesema *Allah Subhanah wa Taala katika* kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَٱسْجُدْ وَٱقْتَرِب﴾

Wasjud Waqtarib - Na Sujudu Na Ukaribie*(Surat Al Aalaq 96:19)*

Ambapo tunapoziangalia Aya hizi basi tunaona kua zinawaamrisha Wale Walioamuamini *AllahSubhanah wa Ta'ala* kua Warukuu na Wasujudu, kwani kufanya hivyo hua ni Kumuabudu Mola wao. Na kisha Wafanye Mema ili wapate kua ni wenye Kufuzu

.

Na bila ya shaka kama tunavyojuakua pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaponadia kwa *kusema Ya Ayyuha Aladhina Amanuu* yaani Enyi wale ambao Mlioamini basi hua kitakachofuatia baada ya hapo kama atajitaja yeye basi hua hatumii Jina Tukufu la Allah, bali hutumia Jina la Tukufu la Rabb yaani Rabbakum - Mola wenu.

Na anaponadia kwa kusema *Ya Ayyuha Al Nasu* yaani Enyi Watu na kisha akajitaja kwa kujihusisha yeye basi hutumia Jina Tukufu la Allah.

Kwa Sababu Allah ni Mungu Muumbaji wa Kila kitu na ni msimamizi wa Kila mtu anaemuamini na asiemuamini.

Ambapo neno Rabb lenye kumaanisha Mlezi aliekua Bora wa Kusimamia Kila kitu tangu mwanzo wake hadi mwisho wake basi hulitumia kwa Waumini wake kuwaonesha namna anavyowajali na kuwapenda katika Malezi yake Waumini wake hao na hivyo kua ni mwenye kuwaonesha Njia nzuri na bora zaid ya Kumkaribia yeye.

Kama kwenye Amrisho la Aya hii ya Surat Al Hajj 22:77 ambalo linafafanuliwa zaid na aya hii ya Surat Al Aalaq kwa kusema kua Kusujudu kwenu ndio Njia nyepesi na ya Haraka zaid ya kunikaribia mimi Mola wenu.

Na kama alivyosema Abu Hurayrah*Radhi Allahu Anhu*katika Hadith isemayo kua:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ أَقْرَبُ مَا يَكُونُ الْعَبْدُ مِنْ رَبِّهِ وَهُوَ سَاجِدٌ فَأَكْثِرُوا الدُّعَاءَ

Amesema *Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu kua*: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ukaribu wa mja anaoweza kua nao Kwa Mola wake ni Anapokua kwenye Sujud, hivyo Zidisheni Dua (kwenye Sujud)(*Sahih Muslim)*

Naam kama ilivyokua kwa Nia ya Sala, *Takbirat Al Ihram*, Kisimamo cha Sala, Usomaji wa Surat Al Fatiha, Rukuu na Ijtidal kua ni vitu vyenye umuhimu sana katika ukamilishaji wa Ibada ya Sala ya Mtu kwa sababu vitu hivyo ni Miongoni maa nguzo za Sala Basi ndivyo ilivyopia Sujud.

Kwani Sujud ni Nguzo ya Saba ya Sala ambayo ni yenye Kufuatia baada ya Kisimamo cha kutoka kwenye Rukuu ambapo baada ya Kisimamo hicho basi ili Mtu anaesali awe ni mwenye kuingia kwenye Sujudu hua inambidi kusema Allahu Akbar na moja kwa moja akiwa ni mwenye kuelekea chini katika Kitendo cha Kusujudu.

Naamesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **‘Mimi nimemuona *Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* alipokua akisimama Kusali alikua akinyanyua mikonoyake hadi kwenye Mabega yake, na hufanya hivyo tena pale anaposema *Takbir Al Itiqaal* ya Kurukuu na anaponyanyua Kichwa chake kutoka katika Rukuu na alikua akisema *Sami Allahu Liman Hamida* lakini hakua akinyanyua mikono katika wakati anapoenda katika Sijda**.

Kwani kitendo cha Kusjudu ni kitendo Muhimu sana katika Sala mithili ya Sala yenyewe na hivyo kupewa Darja ya kua ni Nguzo ya Sala, kwa maana hio basi Sala haiwezi kua Sala bila ya kua na Sujud ndani yake, kama inavyosema Hadith yetu kua:

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ حُجْرٍ، أَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ جَعْفَرٍ، عَنْ يَحْيَى بْنِ عَلِيِّ بْنِ يَحْيَى بْنِ خَلاَّدِ بْنِ رَافِعٍ الزُّرَقِيِّ، عَنْ جَدِّهِ، عَنْ رِفَاعَةَ بْنِ رَافِعٍ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم بَيْنَمَا هُوَ جَالِسٌ فِي الْمَسْجِدِ يَوْمًا قَالَ رِفَاعَةُ وَنَحْنُ مَعَهُ إِذْ جَاءَهُ رَجُلٌ كَالْبَدَوِيِّ فَصَلَّى فَأَخَفَّ صَلاَتَهُ ثُمَّ انْصَرَفَ فَسَلَّمَ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَقَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَرَجَعَ فَصَلَّى

ثُمَّ جَاءَ فَسَلَّمَ عَلَيْهِ فَقَالَ " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَفَعَلَ ذَلِكَ مَرَّتَيْنِ أَوْ ثَلاَثًا كُلُّ ذَلِكَ يَأْتِي النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم فَيُسَلِّمُ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَيَقُولُ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَخَافَ النَّاسُ وَكَبُرَ عَلَيْهِمْ أَنْ يَكُونَ مَنْ أَخَفَّ صَلاَتَهُ لَمْ يُصَلِّ فَقَالَ الرَّجُلُ فِي آخِرِ ذَلِكَ فَأَرِنِي وَعَلِّمْنِي فَإِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ أُصِيبُ وَأُخْطِئُ . فَقَالَ " أَجَلْ إِذَا قُمْتَ إِلَى الصَّلاَةِ فَتَوَضَّأْ كَمَا أَمَرَكَ اللَّهُ ثُمَّ تَشَهَّدْ وَأَقِمْ فَإِنْ كَانَ مَعَكَ قُرْآنٌ فَاقْرَأْ وَإِلاَّ فَاحْمَدِ اللَّهَ وَكَبِّرْهُ وَهَلِّلْهُ ثُمَّ ارْكَعْ فَاطْمَئِنَّ رَاكِعًا ثُمَّ اعْتَدِلْ قَائِمًا ثُمَّ اسْجُدْ فَاعْتَدِلْ سَاجِدًا ثُمَّ اجْلِسْ فَاطْمَئِنَّ جَالِسًا ثُمَّ قُمْ فَإِذَا فَعَلْتَ ذَلِكَ فَقَدْ تَمَّتْ صَلاَتُكَ وَإِنِ انْتَقَصْتَ مِنْهُ شَيْئًا انْتَقَصْتَ مِنْ صَلاَتِكَ " . قَالَ وَكَانَ هَذَا أَهْوَنَ عَلَيْهِمْ مِنَ الأَوَّلِ أَنَّهُ مَنِ انْتَقَصَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا انْتَقَصَ مِنْ صَلاَتِهِ وَلَمْ تَذْهَبْ كُلُّهَا . قَالَ وَفِي الْبَابِ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ وَعَمَّارِ بْنِ يَاسِرٍ . قَالَ أَبُو عِيسَى حَدِيثُ رِفَاعَةَ بْنِ رَافِعٍ حَدِيثٌ حَسَنٌ . وَقَدْ رُوِيَ عَنْ رِفَاعَةَ هَذَا الْحَدِيثُ مِنْ غَيْرِ وَجْهٍ

Amesema Rifaa Ibn Rafii *Radhi Allahu Anhu* kua, Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua amekaa Msikitini nasi tukiwa pamoja nae. Na mara akaingia Bedui alieonekana kama kwamba anataka Kusali, na Kasali Sala yake kwa Ufupi sana, na kisha alipomaliza akanyanyuka na kumsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akitikia *Wa Alaykum Salaam* na kisha akasema: 'Rudi ukasali tena, kwani kwa hakika wewe Hujasali.'**

Hivyo yule Bedui akarudia Kusali kisha akamsalimia tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akamuitikia na kisha akamwambia Rudia tena kusali kwani kwa hakika wewe hukusali.

Bedui akarudia Kusali na kurudishwa kama mara mbili tatu na kila mara *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anamwambia Arudie kusali.

Tukio hili liliwashtua Sana Masahaba kutokana na kuona kua kumbe Mtu anaesali Sala fupi hua hana sala.

Lakini mwishowe Bedui huyo akasema: 'Ya Rasul Allah, basi bora nifundishe kwani mimi ni Ibn Adam mwenye kujihangaisha na kukosea.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Sawa Unapotaka kusali tia Udhu kama alivyokuamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kisha Adhini na Kimu Sala pia.**

Kisha Ukisali basi Soma Qur'an kama unajua na kama hujui basi Mtukuze *Allah Subhanah wa Ta'ala,* fanya Dhikr Allah na fanya Tahlil,Kisha Rukuu hadi uwe umetulia kwenye Rukuu yako, kisha Simama Sawia,kisha Sujudu kikamilifu, kisha Kaa kitako hadi uhakikishe kua umepumzika,Kisha Simama na ukifanya hivyo utakua umekamilisha Sala yako, na ukipunguza basi utakua hukuikamilisha Sala yako.

Na Hivyo hua ni bora kuliko kutokamilisha, kwani ikipungua kitu Sala yako basi itakupunguzia Malipo yake lakini hutokosa kabisa.

Hili lilikuwa jepesi kwao kuliko lile la kwanza, kwa sababu mwenye kujiepusha na jambo hilo ameipunguzia Sala yake, lakini hakuikosa Yote. Ambapo amesema Abu Hurairah na Ammar Ibn Yassir, Abu Issa amesema: "Hadithi ya Rifa'ah Ibn Rafi' ni hadithi nzuri." Imepokewa kuhusiana na Ubora wa Hadithi hii kua ni Hadith isiyokua na Shaka.*(Sunan At Tirmidhii)***

KUTANGULIZA CHINI MIGUU AU MIKONO KWANZA KATIKA SUJUD?

❖❖❖

Hivyo kama tunavyoona katika vithibitisho kua Wajibu wa Kusujudu umetajwa ndani ya Qur'an, ndani ya Hadithza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo bila ya shaka Maimam na Wanazuoni wa Madhhab yote ya Kiislam wanakubaliana juu yake.

Na Sujud ya Mtu kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* iwe ndani ndani ya Sala au nje ya Sala, basi hua ina masharti yake ambayo inabidi yatekelezwe, kwani ni kutokana nayo tu basi ndio Sijda husika itaweza kuhesabika kua ni Sijda kwa ajili ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na miongoni mwa Masharti hayo ni kwamba kwanza iwe ni yenye kuambatana na Takbir. Kisha iwe ni yenye kua kutekelezwa na mtekelezaji katika hali kama isemavyo Hadith ya Wail Ibn *Hujair Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:

رَأَيْتُ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم إِذَا سَجَدَ وَضَعَ رُكْبَتَيْهِ قَبْلَ يَدَيْهِ وَإِذَا نَهَضَ رَفَعَ يَدَيْهِ قَبْلَ رُكْبَتَيْهِ

'Nilimuona Mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiweka Magoti yake chini kabla ya kuweka Mikono yake Ardhini katika Wakati ambao alikua Akiajudu, na anaponyanyuka Hunyanyuka kwa kunyanyua mikono yake kwanza kutoka Ardhini kabla ya kunyanyua Magoti yake.'*(Imam Abu Daud, Imam Tirmidhii, Imam An Nasai na Ibn Majah)*

Ambapo Imam Ali Ibn Umar Ibn Ahmad Ibn Mahdi Ibn Masud Ibn Nuuman Al Baghdadi Al Daraqutni akasema kua: **'Sanad ya walionukuu Hadith hii, ni kama ifuatavyo: Yazid (alieinukuu peke yake) ambae amenukuu kutoka kwa Shariq (alienukuu peke yake) ambae amenukuu kutoka kwa Asim Ibn Kulayb, lakini hata hivyo kwa kua Hadith hii ina watu wawili walionukuu peke yao katika Sanad yake basi Hadith hii inahesabiwa kua ni Hadith dhaif.'**

Ambapo juu ya Hatua hizi za kuingia na kutoka kwenye Sujud basi pia kuna Hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:

كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَفْعَلُ ذَلِكَ

'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alipokua akisjudu basi hutanguliza Mikono yake kwanza Ardhini kabla ya Magoti yak**e.'*(Sahih Ibn Khuzaimah)*

Na kua hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua:

إِذَا سَجَدَ أَحَدُكُمْ فَلاَ يَبْرُكْ كَمَا يَبْرُكُ الْبَعِيرُ وَلْيَضَعْ يَدَيْهِ قَبْلَ رُكْبَتَيْهِ

Amesema *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam kua:* **‘Pale mmoja wenu atakapokua anasjudu basi hatakiwi kua ni mwenye kuinama kama anavyoinama Ngamia, bali anatakiwa atangulie mikono yake kwanza kabla ya Magoti.***’(Sunan Al Darimi, Sunan Abu Daud)*

Ambapo amesema kuhusiana nayo hadithi hii Imam Ibn Al Qayim Al Jawziyyah katika kitabu chake cha Zad Al Maad kua: **‘Kuna tatizo katika Hadith hii ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*ambalo ni kua mwanzo wake unapingana na mwisho wake, kwa sababu Hadith hii imekataza kutopiga kuinama kama afanyavyo Ngamia, na kisha kuamrisha kuinama kwa kutanguliza Mikono yetu kabla ya Magoti yetu, wakati Ngamia anapokaa hukaa kwa kutangulia chini kiguu yakeya mbele kwanza kabla ya miguu ya nyuma, na pia hadith hii inaonekana kua ni yenye inqilab yaani yenye kuchanganya katika maneno yake hivyo inawezekana ikawa imekusudiwa kutanguliza Magoti mwanzo kabla ya Mikono’***(Zaad Al Maad)***

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ إِذَا سَجَدَ بَدَأَ بِرُكْبَتَيْهِ قَبْلَ يَدَيْهِ

‘**Alikua Nabii *Salallahu Alayhi wa Salam* anaposujudu hua ni mwenye kuweka kwanza magoti yake chini kabla ya kuweka Mikono yake,’**(*Sharh Ma’ani Al Athaar li Al Tahawi na Qurratu Al Ainayn bi Raf’I Al Yadayn fi Al Salah* li *Al Bukhari*)

Kwani kwa Maana hio basi Juu ya Jambo hili la hatua za Sujud hua lina Mitizamo miwili tofauti. Ambapo mtizamo wa kwanza ni Mtizamo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal n.k ambao wao wanasema kua: ‘**Katika Hatua za Kusjudu basi Kwanza Mtu anatakiwa aweke Magoti chini na kisha ndio Mikono yake.’**

Na pia kuna Mtizamo wa pili ambao ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik Ibn Anas, Imam Al Awzai, Baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Hanbal na wengineo ambao wao Wanasema kua: ‘**Katika Hatua za Kusjudu basi kwanza Mtu anatakiwa aweke mikono yake chini kisha ndio Magoti yake.’**

Na ndio maana akasema Mujaddid Ad Din Imam Abu Abd Allah Muhammad Idris Al Shafii kua: ‘**Hakika Mimi nnapenda Kuianza Sala yangu kwa Takbir na kisha ninaposujudu hupenda kutanguliza Magoti yangu Ardhini kwanza kabla ya Mikono yangu’***(Kitab Al Umm)*

Kwani kuhusiana na mitizamo hii basi kua Hadith nyengine isemayo kua**: ‘Anasema Ismail Ibn Yahya kua:**

كُنَّا نَضَعُ الْيَدَيْنِ قَبْلَ الرُّكْبَتَيْنِ، فَأُمِرْنَا بِالرُّكْبَتَيْنِ قَبْلَ الْيَدَيْنِ

‘**Sisi tulikua tukiweka Mikono yetu kwanza kabla ya Magoti lakini Tukaambiwa kuaTutangulize Magoti kwanza kabla ya Mikono.’***(Imam Ibn Khuzaymah, Imam Al Bayhaqi, Imam Al Baghawi)*

Na ingawa hadith hii inaonekana kua ni dhaifu kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni, lakini kuna Athari ya Kauli au Riwaya ambayo ni yenye kuaminika sana kwa usahihi wake na imenukuliwa na Imam Al Tahawi katika *Sharh Al Maani Al Athari* isemayo kua: **‘Wamesema Masahaba kua Hakika sisi**

Tumehifadhi Namna alivyokua akisali Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* ambapo katika kusali kwake alikua baada ya kurukuu kwake anapoingia kwenye Sujudu alikua akitanguliza chini Magoti yake kabla ya kutanguliza Mikono yake kama vile afanyavyo Ngamia.'*(Sharh Al Maani Al Athari)*

Hivyo anasema Imam Abu Sulayman Hamd Ibn Muhammed Ibn Ibrahim Al Khattabi Al Basti Al Shafii kua: 'I**ngawa Kuna kutokukubaliana baina ya Wanazuoni juu ya Jambo hili lakini wengi sana miongoni mwa Wanazuoni Wanakubaliana kua kuhusiana na Kusjudu basi kwanza Mtu anatakiwa atangulize chini Magoti kabla ya Mikono yake kwani kufanya hivyo hua ni Kukiboresha kitendo cha Kusjudu kwa Usafi na kwa Uzuri zaidi.'** *(Maalim al Sunnah)*

Kwani kwa maana hio basi hatua za Kitendo hiki cha kuingia kwenye Sujud hua kinajulikana kama *Muktabar Al Khilaf* yaani Kitendo kinachopelekea kukubalika kuwepo kwa Makubaliano ya Kutofautiana ndani yake kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni.

Na hivyo amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakkariyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Hakuna uwazi juu ya kua ni Mtizamo upi uliokua Sahih katika Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya Kitendo hiki Lakini katika Madhhab yetu basi ni Sunna kuanza kuweka Magoti chini katika kuingia kwenye Kusujudu na kisha ndio unaweka Mikono, kisha Paji la Uso na kisha ndio Pua.'**(*Al Majmuu)*

Ambapo anasema Imam Abd Al Aziz Ibn Marzuq Al Tarifi Al Shafii kua: 'K**una hoja nyingi sana kutoka kwa Wanazuoni kuhusiana na Jambo hili, na hivyo Watu wanatakiwa Kusali Sala zao kwa kuchagua njia moja kati ya Mbili hiz**i. **Ambayo itakua Rahisi kwa Mtu husika (yaani aidha kwa kutanguliza Magoti kwanza au kwa kutanguliza Mikono kwanza Ardhini katika Kusjudu)**. **Kwani Muhimu ni Kusjudu, na hii kwa sababu Watu wametofautiana kuna Wenye Miili Mikubwa na Minene na kuna wenye Miili myembamba, hivyo Mtu afanye kile kilichokua Rahisi kwake katika Kuingia kwenye Kusujdu**'*(Sifat Salat An Nabii)*

Kwa Maana hio basi haina haja mtu ukamuona Mwenzako anasali kisha katika wakati wa Kusjudu akatanguliza Mikono kwanza kabla ya Magoti, kisha ukaanza kumhukumu, kwa sababu wewe unaweza kutanguliza Magoti kwanza kabla ya mikono.Kwani kwa kua Jambo hili lina hali ya *Muktabar Al Khilaf* basi kila mmoja afanye ilivyokua rahisi kwake kutekelezeka kulingana na Maumbile yake na pia kulingana na Mtizamo wa Madhhab anayofuata.

Naam hivyo tunapozungumzia kuhusiana namna ya kuingia kwenye Hatua ya Sijda ya Sala baada ya kutoka kwenye Kisimamo kilichofuatia baada ya Rukuu basi ni kama walivyosema Wanazuoni kua inaruhusika kutanguliza Magoti kuanza kugusa Ardhini kisha ndio Mikono ambao ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni na pia inaruhusika kutanguliza mikono kwanza kabla ya Magoti.

Tumalizie na *Hadith Gharib* yenye *Isnad sahih* iliyonukuliwa na Imam Qasim Al Saraqusti ambae anasema kua: **'Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Haitakiwi kwa Mtu kusujudu kama anavyosujudu Ngamia aliekua akikimbia.'** Kwani Haitakiwi kwa mtu mwenye kusujudu kujitupa kama anavyojitupa Ngamia aliekimbia ambae hajafungwa kamba, hua ni mwenye kuenda chini kwa haraka na vishindo, bali Mtu anatakiwa asijudu kwa utaratibu kwa kuanza kutanguliza Ardhini Magoti kwanza kisha Mikono kisha Paji la Uso na Pua

UMUHIMU WA KUGUSISHA PAJI LA USO NA PUA ARDHINI

❖❖❖

Tumetaja Paji la Uso na Pua kwa sababu kufanya hivyo ndio hua kunakamilisha kitendo cha Sujud kama alivyosema*Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

أُمِرْتُ أنْ أسْجُدَ علَى سَبْعَةِ أعْظُمٍ علَى الجَبْهَةِ، وأَشَارَ بيَدِهِ علَى أنْفِهِ واليَدَيْنِ والرُّكْبَتَيْنِ، وأَطْرَافِ القَدَمَيْنِ ولَا نَكْفِتَ الثِّيَابَ والشَّعَرَ

‘**Nimeamrishwa mimi Kusujudu kwa Kutumia Mifupa Saba ambayo ni Paji la Uso,(Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akagusa na Pua yake na kisha akasema) Na Mikono, Magoti na Ncha za Vidole vya Miguuna nisiondoe Nguo wala Nywele.’***(Sahih Bukhari)*

Hivyo baada ya Mtu anaesali kuingia katika hali ya Kusjudu iwe kwa kufikia Magoti mwanzo au Mikono na Kusjudu basi anatakiwa ahakikishe kua Sehemu 7 za Mifupa ya Mwili wake iwe ni yenye kugusa Ardhi ya Sehemu anayosujudia Ambayo ni Paji la Uso na Pua,Viganja Vya Mikono yote Miwili,Magoti yote mawili na Vidole vyote vya Miguu huku viungo vyote hivyo vikiwa ni vyenye kuelekea Kibla.

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakkariyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: ‘**Kulingana na Hadithi hii ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi inatudhirishia kua Kuna Sehemu za Viungo 7 za Kusjudia, na Hivyo Mtu mwenye Kusjudu anatakiwa Lazima Asjudu kwa kutumia Sehemu 7 hizo ambazo ni Paji la Uso na Pua, Viganja vya Mikono, Magoti na Ncha za Vidole vya Miguu Na Paji la Uso linatakiwa Liwe Wazi lisifunikwe na Kitu katika Wakati linapogusa sehemu ya Kusujudia na pia Sehemu ya Ncha ya Pua.’**

‘Hivyo kama akisjudu huku Paji lake la Uso na Pua ikigusa sehemu anayosujudia basi Sijda yake hua sahih lakini kama hakugusisha Paji la Uso basi Sijda yake ni Batili. **Na huu ndio Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Madhhab ya Imam Malik na wengineo. Na wengi miongoni mwa Wanazuoni wanazungumzia hadithi hii kulingana na maneno yake yasemayo kua Vinugo vinavyotakiwa kusujudia ni 7 lakini kama ikihesabiwa na Pua basi hua ni Vinane, hivyo Kugusisha Pua Ardhini katika wakati wa Kusujudu hua ni Sunna’** *(Sharh Sahih Muslim)*

Na amesema pia Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:

إذَا سَجَدْتَ فَمَكِّنْ جَبْهَتَكَ من الارض ولا تنقر نَقْرًا

‘**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Unaposujudu basi Gusisha Paji lako la Uso Ardhini, Usiwe ni mwenye Kuinama.’**

Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idriams Al Shafii anasema kua: ‘**Kama ikiwa ni sehemu tu ya Paji la Uso ndio linalogusa chini katika Kusjudu basi hali hio hua ni Makruh lakini hua inakubalika kwa sababu huko hua pia ni Kusujudia Paji la Uso**. **Na kama ikiwa Paji la Uso**

linagusa juu ya Kitu ambacho kimezuia Paji la Uso kugusa chini basi Sijida hio hua haihesabiki.'*(Kitab Al Umm/Al Majmuu Sharh Al Muhaddhab)*

Kwa maana hio basi Kuhusiana na Paji la Uso basi Sijda hua inakubalika pale Mtu anapokua Paji la Uso na Pua inapokua vinagusa chini, na hata kama Mtu tuseme atakua amevaa Kofia au Kilemba ambacho kitafika mpaka juu ya Macho na Kufunika Paji la Uso basi hii hua ni Makruh.

Lakini tuseme labda Mtu atakua amevaa *Pullover* au *Hoodies* yaani Nguo zenye Kofia kama Makoti ya Baridi,au Kanzu za Kimoroco, ambapo kama Kofia yake itakua inamfuata na Akisimama inabakia Mgongoni au Mabegani, na akirukuu inasogea Shingoni na akisujudu Inamfunika Paji la Uso basi hii hua haikubaliki katika Sala. Ila Kofia au Kilemba au Hijab hua Inakubalika kwa sababu Nguo hio hua haichezi kwa kujitegemea peke yake kulingana na Vitendo vyake bali hua imeandamana na kushikamana na Kichwa na haijitegemei peke yake.

Kwani amesema *Imam Al Muhaqqiqin Al Faqih Imam Ibn Hajar Al Haytami* kua: '**Sharti hili la Kutosujudu juu ya Kitu alichokichukua au kukibeba hua linashikama na kitu ambacho kitakua kinacheza katika Hatua zake za Kuinama na Kuinuka, hivyo kama mtu atasujudia juu yake kitu hicho na anajua kua hivyo hua haifai basi Sala yake Mtu huyo inabatilika Na Kama ikiwa Mtu huyo hakukusudia au alikua hajui basi inambidi Kuirudia Sujud hio'***(Manhaj Al Qawim)*

Na hivyo tunajaribu kuiangalia Sijda katika mitizamo tofauti ili tupate kuifahamu zaid na hii ni kwa Sababu katika Kila Sala mna Sijda zisizopungua 4, na hivyo ukiikosea ya kwanza tu basi unakua umezikosea zote na umeikosa Sala nzima.

Kwa sababu anasema Al Hafidh Imam Abu Muhammad Abd Al Adhim Ibn Abd Al Qawi Zaki Ad Din Al Mundhiri Al Shafii kua: '**Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua**: **Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kwa Hakika Mtu anaweza akawa anasali kwa mda wa Miaka 60, lakini Isikubaliwe Sala yake hata Moja kwa Sababu ya Kukamilisha Rukuu bila Kukamilisha Sujud, au Kukamilisha Sujud bila kukamilisha Rukuu.'** *(Sahih Al Targhib wa Tarhib)*

Na hivyo ili tuweze kujua na kuweza Kukamilisha Sujud basi inabidi tuangalie kila kiungo kati ya viungo 7 vikivyotajwa kwenye Hadith yetu inayohusiana na Sujud.Hivyo tunaendelea na kuhusiana na Kiungo cha Kwanza kilichotajwa na Hadith yetu ambacho ni Paji la Uso na hii pia ni kwa sababu amesema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Hana Sala yule ambae Pua yake haigusi Ardhi kama vile ligusavyo Paji lake la Uso.'***(Imam Bukhari, Imam Ad Daraqutni, Imam Al Hakim, Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo kwa upande wa Al Imam, Al Hafidh Al Thiqah, Al Rahhal Al Jawwal Al Muhaddith Al Islam Abu Qasim Sulayman Ibn Ahmad Ibn Ayyub Ibn Mutayyir Al Lakhmi Ash Shami At Tabarani basi yeye anasema kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**'**Sala ya Mtu ambae Haweki chini Pua yake pamoja na Paji lake la Uso kwenye Ardhi pale anaposujudu hua ni Batili**.'*(Imam At Tabarari)*

Hivyo hadhithi hizi zinatuonesha umuhimu wa kugusisha Paji la Uso na Pua Ardhini katika wakati wa Kusujudu. Ambapo Katika Hadith yetu ya sehemu za Viungo 7 vya kusujudia basi tumeona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* alihesabu alitaja Paji la Uso na kisha akaiashiria na Pua yake kumaanisha kua Sehemu Mbili hizo zinahesabika kua ni Kiungo kimoja cha Uso, kama vile ambavyo inavyohesabika Kiganja cha Mkono kua ni pamoja na Vidole vyake.

Ambapo anasema *As-hab Al Wujuh wa* Madhhab ya Imam Al Shafii, Imam Abu Zayd Muhammad Ibn Ahmad Al Marwazi Ibn Abd Allah Al Fashani Al Shafii ambae ni mwanafunzi wa Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Ahmad Al Marwazi Al Shafii. Imam Abu Zayd Al Marwazi ni Imam mwenye Sifa za Upekee katika Kua na Ilm kubwa sana yenye kutisha kuhusiana na tofauti ya Mitizamo baina ya Masahaba Wanazuoni na Tabiina Wanazuoni.

Hivyo anasema Imam Abu Zayd Al Marwazi kua: '**Kugusisha Pua Ardhini katika wa Kusjudu si Kwenye Kupendekezwa tu, bali ni Wajib.**'*(Sharh Muhadhdhab)*

Na Imam Abu Zayd Al Marwazi amesema hivi kwa sababu: '**Kuna baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafiina wengineo wamesema kua kuigusisha Pua Ardhini kwenye Sujud hua sio Lazima, bali kunapendekezwa tu, na hii ni kwa sababu neno lililotumika katika hadithi ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* ni:**

جَبْهَت

Yaani Paji la Uso na halimaanishi Pua, na pia Dalili inayohesabiwa kua na nguvu zaidi katika Hukmu hua ni Kitendo cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na wala si Kauli *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kwa hivyo ujumuishwaji wa Pua katikaSujudu hua si lazima kua na uzito wa kiwango wa kile kilichooneshwa katika Dalili, na kwa upande wa pili basi kile kinachoamrishwa kwa Vitendo vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*hua si lazima kua na kiwango wa kile kinachoamrishwa kwa Kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na pia, kuhusiana na kitendo cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuweka mkono juu ya Pua yake huenda ikawa ilitokea baada ya kuweka kwenye paji la uso wake. Ambapo hili liko wazi katika Hadith iliyonukuliwa na Imam An Nasa'i katika Sunan yake. Kwa hivyo kugusa Pua kunaweza kuwa kwa bahati mbaya kunakotokana na wakati wa kuinua mkono baada ya kugusa Paji la Uso. Ni kawaida sana kwa neno Paji la Uso kuambatana na dalili kwenye Paji la Uso halisi. Kwani kusema Paji la Uso na kisha kuashiria Pua hua sio kawaida kabisa.

Hata hivyo tunapomuangalia Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi katika Sharh Al Muhadhdhab Juzuu ya 3 katika ukurasa wa ukurasa wa 424 basi tunaona kua anaungana mkono na *As-hab Al Wujuh wa* Madhhab ya Imam Al Shafii, Imam Abu Zayd Muhammad Ibn Ahmad Al Marwazi Ibn Abd Allah Al Fashani Al Shafii kusema kua: '**Kugusisha Pua Ardhini katika wa Kusjudu si Kwenye Kupendekezwa tu, bali ni Wajib.**'na kusema kua: **'Mtizamo huu ni wenye kua na nguvu kulingana na vithibitisho.'**(*Sharh Muhadhdhab)*

Na hii pia ni kama tunavyooneshwa katika Hadith ifuatayo katika Sunnan At Tirmidhii kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ، بُنْدَارٌ حَدَّثَنَا أَبُو عَامِرٍ الْعَقَدِيُّ، حَدَّثَنَا فُلَيْحُ بْنُ سُلَيْمَانَ، حَدَّثَنِي عَبَّاسُ بْنُ سَهْلٍ، عَنْ أَبِي حُمَيْدٍ السَّاعِدِيِّ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم كَانَ إِذَا سَجَدَ أَمْكَنَ أَنْفَهُ وَجَبْهَتَهُ مِنَ الأَرْضِ وَنَحَّى يَدَيْهِ عَنْ جَنْبَيْهِ وَوَضَعَ كَفَّيْهِ حَذْوَ مَنْكِبَيْهِ . قَالَ وَفِي الْبَابِ عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ وَوَائِلِ بْنِ حُجْرٍ وَأَبِي سَعِيدٍ . قَالَ أَبُو عِيسَى حَدِيثُ أَبِي حُمَيْدٍ حَدِيثٌ حَسَنٌ صَحِيحٌ . وَالْعَمَلُ عَلَيْهِ عِنْدَ أَهْلِ

الْعِلْمِ أَنْ يَسْجُدَ الرَّجُلُ عَلَى جَبْهَتِهِ وَأَنْفِهِ فَإِنْ سَجَدَ عَلَى جَبْهَتِهِ دُونَ أَنْفِهِ فَقَدْ قَالَ قَوْمٌ مِنْ أَهْلِ الْعِلْمِ يُجْزِئُهُ . وَقَالَ غَيْرُهُمْ لاَ يُجْزِئُهُ حَتَّى يَسْجُدَ عَلَى الْجَبْهَةِ وَالأَنْفِ

AmesemaMuhamamd Ibn Bashar kua: Amesema Abu Amir Al Aqadiyu kua Amesema Fulayh Ibn Sulayman kua Amesema Abbas Ibn Sahil kutoka kwa Abu Humayd Al Saadi amesema kua: *Radhi Allahu Anhu kua: '**Wakati Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alipokua akisjudu, basi alikua akigusanisha Pua yake na Paji lake la Uso Ardhini**. **Na alikua alikua si mwenye Kujibana Mikono yake na alikua akiiweka viganja Vyake Sambamba na usawa wa Mabega yak**e.'*(At Tirmidhi)*

Kisha Imam At Tirmidhii anaendelea kusema kua: Hadith hii pia imenukuliwa na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na Wail Ibn Hujayr *Radhi Allahu Anhu na* Abu Said Al Khudhry *Radhi Allahu* Anhu, na hii Hadith ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* ni Hadith ambayo ni Hasan SahihNa kutokana nayo basi Wanazuoni wanasema kua Paji la Uso na Pua ya Mtu anaesujudu ni lazima Iguse Chini. **Lakini kama Mtu akisjudu bila ya Pua yake Kugusa Ardhini basi Sala yake hua haibatiliki, ambapo pia kuna Wanzuoni Wasemao kua Sala ya Mtu asiegusisha Chini Pua yake na Paji lake la Uso katika Wakati wa Kusjudu hua ni Batili***(Sunnan At Tirmidhii)*

Ambapo anasema piaSayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafikua: '**Ni Wajibu kwa sehemu Ngumu ya Pua kugusa Ardhini katika Wakati wa Kusujudu. Hivyo hua hairuhusiwi kwa Mtu kujitosheleza katika Kusujudu kwake kwa kugusisha Ncha tu ya Pua yake Ardhini.'***(Radd Al Mukhtar)*

Na kwa upande mwengine basi amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua:

رَأَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَسْجُدُ بِأَعْلَى جَبْهَتِهِ عَلَى قِصَاصِ الشَّعْ

'Miminilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisjudukwa kuweka sehemu ya Juu ya mwisho kabisa ya Uso wake na MwishoniMwa Ukingo wa Nywele zake*. '(Imam Ad Daraqutni)*

Ambapo anasema Imam Ahmad Ibn Abd Rahman Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Ama kuhusiana na Pua katika wakati wa Kusjudu basi kuna Hadith mbili juu yake**. **Hadith ya kwanza inatilia Mkazo kuigusisha Ardhi katika wakati wa Kusujudu.'**

'Na hadith ya pili inaonesha kua Hua Si Wajibu Kusujudia, ambapo huu ndio Mtizamo wa Imam Ataa, Imam Tawus, Imam Iqrimah, Imam Hasan Al Basr, Imam Ibn Siriin Imam Al Shafii,Imam Abu Thawr na Wanafunzi wawili wa Imam Abu Hanifa(Imam Abu Yusuf na Imam Muhammad Ash Shaybani) na hii ni kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua : 'Nimeamrishwa Kusjudia Viungo 7 vya Mwili na hakuitaja PuaNa pia kua Hadith ya Jabir *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisujudu kwa kutumia sehemu ya Juu kabisa ya Paji lake la Uso karibu na Nywele zake.''*(Al Mughni)*

Hivyo kama tulivyoona kua kuna mitizamo tofauti kuhusiana na Kugusisha Pua Ardhini pamoja na Paji la Uso kwenye Ardhi katika Wakati wa Kusjudu.Na hii ni kulingana na Vithibitisho vya Hadith Mbali Mbali ambazo zimewapelekea Wanazuoni kuhitimisha kua Kugusisha Pua Ardhini katika Sijda hua ni

Wajib hivyo ni Lazima kugusisha na wengine kusema kua hua ni Sunna na hivyo ukifanya unapata Thawabu zaidi na kama hukufanya basi huongezewi wala Hupinguziwi.

Hivyo kwa mtizamo wangu mimi mwenye Dhambi ngingi zaid basi ni bora kushikamana na Mtizamo wa Imam Abu Zayd Muhammad Ibn Ahmad Al Marwazi Al Shafii, yaani kua ni Wajib ili kuchuma Malipo ya Thawabu zaidi na kuipandisha Darja zaidi Sala kutokana kuigusisha Pua Ardhini katika Kusjudu.

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua**: 'Wanazuoni Wanakubaliana kua Kuweka Paji la Uso Moja kwa Moja Ardhini katika Wakati wa Kusjudu hua ni Jambo lenye Malipo Makubwa San**a'*(Al Majmuu)*

Lakini hata hivyo kuna baadhi ya Wakati basi Jambo hili hua haliwezekani na hii ni kwa sababu Ili ufanikishe jambo hili basi inabidi Usiwe ni Mwenye Kuvaa Kofia, Kilemba n.k. Au Ukivaa basi inabidi Usiivute sana chini hadi ikafunika Paji lote la Uso.

Ambapo kwa Upande mwengine, hua inatokea Dharura, kwa Mfano Mtu anapokua Anasali katika Sehemu yenye Jua kali tuchukulie Mfano katika Wakati wa Sala ya Ijumaa ambapo baadhi ya Miskiti watu hua wanasali hadi Barabarani huku Jua likiwa Kali Sana kiasi ya kua Linaunguza kuanzia Nyayo hadi Paji la Uso katika wakati wa Kusjudu.

Na kuna baadhi tuseme wanajikuta Wanasali kwemye Kokoto, hivyo kwanza Jua halafu Juu ya Kokoto ambazo baadhi hua yana Ncha, hivyo Jee katika hali kama inakuaje?.

Wakati amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

إذا سجدت فمكن جبهتك ولا تنقر نقرا

'**Unaposujudu basi weka Uso wako kwenye Ardhi na kisha Usiuondoe kwa Haraka.'***(Imam Ibn Hibban)*

Na akasema *Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din* Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Haitoshelezi kwa Paji la Uso kua ni lenye Kugusa kwa juu juu tu ya Ardhi ambayo mtu anaesali hua anasujudia, bali inatakiwa Kichwa chake kithibitishe kwa kuwepo kwa Uzito wake na Shingo ihisi kua Kichwa Kimekaa na Kimetulia hasa juu ya Sehemu ya Kusujudia Na wala isiwe kinagusa Tu sehemu hio**. **Hivyo kama mtu anasjudu juu ya Sehemu iliyotandikwa, labda kwa Pamba (Zulia) au Majani Makavu (Jamvi, Mkeka) basi anatakiwa aweke Kichwa chake kiasi ya kua uzito wake utadidimiza Pamba hio na kuacha athari ambayo kama Kwa mfano ingekua kumewekwa Mkono chini ya Pamba hio basi mkono huo uhisi athari hio ya Sujudu, na kama haikua hivyo basi hua haitoshelezi Sujudu yake hio.**'(*Al Majmuu)*

Ambapo kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab Ya Imam Malik basi wao wanasema kua: '**Inatosheleza kwa Mtu anaesali kuweka Paji la uso wake juu ya Ardhi bila ya Kudidimiza Sana kwenye Ardhi hadi ikawa inamuathiri Uso wake, kwani Wafanyavyo Hivyo ni Wajinga wasiojua na Wanawake wenye Udhaifu.'** *(Sharh Al Kifayat Al Taalib mam Ali Ibn Ahmad Ibn Mukarram Allah Al Adaw Al Maliki)*

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Saad Ibn Abi Waqqas *Radhi Allahu Anhu* ambae yeye amesema kua: '**Mtu hatakiwi Augandamize Sana Uso wake Ardhini, kwani kufanya hivyo hua**

haipendekezwi, na ni Wajinga tu ndio wafanyao Hivyo na Wanawake wenye Udhaifu.'*(Imam Al Zarqani katika Sharh Ala Mukhtasar Al Khalil)*

Na anasema Imam Muhammad Ibn Muhammad Ibn Arafah Al Warghami Al Maliki kua: '**Imam Malik alikua ni mwenye Kusema kua Haipendezi kudidimiza Kichwa kwenye Sehemu ya Kusujudia katika wakati anaosujudu mtu.'***(Mukhtasar Al Fiqh Al Maliki)*

Hivyo hio ni baadhi ya Mifano ya Mitizamo ya Wanazuoni kuhusiana na namna kinavyotakiwa Kichwa na Paji la Uso katika Sujud, ambayo ndio inatutayarishia namna ya kukabiliana na Hoja yetu kuhusiana na Kusujudu Juu ya sehemu zinazoumiza wakati ukiwa katika Sala.

Kwani anasema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:

كُنَّا نُصَلِّي مَعَ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، فَيَضَعُ أَحَدُنَا طَرَفَ الثَّوْبِ مِنْ شِدَّةِ الحَرِّ فِي مَكَانِ السُّجُودِ

'**Sisi tulikua tukisali pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na baadhi miongoni mwetu walikua wakiweka sehemu za pembeni za Nguo zao katika sehemu ya Kusujudia kwa sababu ya Ukali Joto la Jua.'** *(Sahih Bukhari)*

Na akasema tena Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* katika hadith ifuatayo:

حَدَّثَنَا مُسَدَّدٌ، حَدَّثَنَا بِشْرٌ، حَدَّثَنَا غَالِبٌ، عَنْ بَكْرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ ـ رضى الله عنه ـ قَالَ كُنَّا نُصَلِّي مَعَ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فِي شِدَّةِ الْحَرِّ، فَإِذَا لَمْ يَسْتَطِعْ أَحَدُنَا أَنْ يُمَكِّنَ وَجْهَهُ مِنَ الأَرْضِ بَسَطَ ثَوْبَهُ فَسَجَدَ عَلَيْهِ.

'**Sisi tulikua tukisali pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Wakati ambao Jua lilikua Likiunguza, kiasi ya Kua kama Mtu hakuwa ni mwenye kuweza kuweka Paji lake la Uso kwenye sehemu anayosujudia Ardhini basi, alikua akitandaza Nguo zake na Kusujudia Juu yake.'***(Sahih Bukhari)*

Naam..hizi ni miongoni mwa Hadtih ambazo zinatuonesha namna Masahaba walivyokua wakitafuta Njia za kuwawezesha Kutekeleza Majukumu yao Mbele ya Mola wao mbali ya kua na hali ya Ugumu wa Mazingira katika utekelezaji wa Majukumu hayo Wakati wao.

Na hii ni kwa Sababu baadhi ya Wakati walikua Wakisali Jangawani kwenye Mchanga Uliopigwa na Jua Kali Kali kwa Masaa kadhaa na hivyo kua ni wenye Kuunguza, Nyayo na Nyuso zao. Kwa upande mmoja tunapoangalia hali hii basi katika mazingira yetu leo hii hua tunakutana nayo kwa wale wanaosali Barabarani katika Sala za Siku ya Ijumaa.

Kwani anasema Imam Hasan Al Basr kua:

كان أصحاب رسول الله صلى الله عليه وسلم يسجدون وأيديهم في ثيابهم، ويسجد الرجل منهم على عمامته.

‘**Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua Wakisujudu huku mikono yao ikiawa Imezungurushiwa kwa nguo zao na baadhi yao awlikua wakisujudu juu ya Vilemba vya**o.’*(Imam Al Bayhaqi li Sunnan Al Qubra)*

Ambapo Kauli hii ya Imam Hasan Al Basr inatuonesha pia kua Mbali ya kua Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua na Ugumu zaidi yetu katika Utekelezaji wa Ibada kulingana na Mazingira yao, lakini hata hivyo Ugumu huo wa Kimazingira haukuwazuia kutotimiza Majukumu yao Mbele ya Mola wao.

Na Masahaba hawakufanya haya katika Nyakati za Jua kali tu bali pia walifanya katika kipindi cha Baridi kali. Na kutokana na Ucha Mungu wao basi Masahaba *Radhi Allahu Anhu* walikua si wenye kupenda kufanya hivyo, kwa sababu wao walikua ni wenye kujua Uzito na Thamani ya Kusujudia juu ya Ardhi kwa kuweka Paji la Uso moja kwa moja juu ya sehemu ya Ardhi husika anayoisujudia na kufahamu kua kila unapopata ugumu katika kufanya Ibada basi ndio malipo yanapokua makubwa zaidi.

Na ndio maana kwa upande wa ‘**Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua anachukia sana kuweka Kitu Juu ya Ardhi ya sehemu anachosujudia.’***(Musanaf Ibn Abi Shaybah)*

Kwani alikua akiamini kua Kila anayopata tabu na shida katika Kufanya Ibada yake basi ndivyo anavyofanikkwa kulipwa Malipo Makubwa zaidi: ‘**Ambapo hali hii alikua nayo pia Imam Muhammad Ibn Sirin ambae nae pia alitangazia kua hapendi Kusujudia juu ya Kilemba.’** *(Musanaf Ibn Abi Shaybah)*

Kwani Sijda ili ihesabiwe kua ni Sujud Basi moja kati ya Masharti yake ni kua lazima ipatikane Utulivu ndani yake. ‘**Kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam***kua:

إذا سجدت فمكن جبهتك ولا تنقر نقرا

‘Unaposujudu basi Weka Kichwa chako Kwenye Ardhi na usikiondoe kwa Haraka.’*(Imam Ibn Hibban)*

Ambapo anasema Al Qadhi, Al Faqih, Az Zahid Al Wazir Imam Abu Tayyib Shihab Ad Din Ahmad Ibn Al Husayn Ibn Ahmad Abu Shujaa Al Asfahani Al Shafii kua: ‘**Kama Mtu atanyanyua Kichwa chake kutoka katika Sujud kwa sababu tu ya kua ni mwenye kuogopa Kitu, basi hio Sijda yake hua Haijatosheleza na hivyo hua ni lazima kwake Kurudi kwenye Sijida hio.’** *(Al Iqana Fii Hal Al Faath Imam Abu Shujaa)*

Naam.tufahamishana kuhusiana na Ibada ya Sala ambayo ndani yake mna Kitendo kitukufu cha Kumsujudia Muumba wetu ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Na kwa kua hiki ndio kitendo pekee kinachomplekea Kiumbe kua na Ukaribu zaid na Mola wake basi ni wajibu wetu kukijua kwa undani ili tupate kufanikisha haya ya Karibu zaid mawasiliano baina yetu na Mola wetu.

Na kwa kua katika kila kitu hua kina wepesi na Ugumu wake kulingana na mazingira ya utokeaji na utekelezwaji wake, basi tunajaribu kuangalia mifano ya namna walivyokua wakikabiliana na ugumu wa Ibada zao kulingana na nyakati zao ili nasi tuweze kutatua changamoto hizo kwa njia ya kufuata Mifano yao.Kwani ni Wajibu wa Kila Muislam kua ni mwenye Kutakiwa kufuata Mifano ya wale walioongoka kutokana na Muongozo wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama ilivyosema Aya:

﴿أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ ۖ فَبِهُدَاهُمُ اقْتَدِهْ ۗ قُل لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرَىٰ لِلْعَالَمِينَ﴾

Ulaika Alladhiina Hada Allahu Fabihudahumu Iqtadih, Kul la as-alulukum aAlayhi Ajran, In huwa illa Dhikraan lil aAlamiina *(Surat Al Anaam 6:90)*

Tafsir: ***Hao Ndio Wale AmbaoWalioongozwa na Allah Hivyo Kuongozwa KwaoKufuateni. Waambie kua Sitaki kutoka kwenu malipo kwani huu si chochote ila niukumbusho kwa Walimwengu.***

Ambapo Kwa Sharia za Kiislam basi Watu hao Wanaotakiwa Kufuatwa baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, basi ni Wanazuoni kwani wao ni Warithi wa Mitume. Na tunapozungumzia Wanazuoni basi Kila Kizazi hua kina Wanazuoni wake, yaani Kuna Wanazuoni Miongoni mwa Masahaba, kina Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*, Zayd Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu*, Ubay Ibn Qaab*Radhi Allahu Anhu, Muadh Ibn Jabbal Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,n.k.*

Miongoni mwa Tabiina, ambapo ndani yake unakutana na Imam Jabir Ibn Zayd, Imam Hasan Al Basr, Imam Muhammad Ibn Sirrin, Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Ibrahim Ibn Adham, n.k.

Miongoni mwa Tabii Tabiina, ambapo ndani yake unakutana na Imam Jafar As Sadiq, Imam Al Zuhri, Imam Sufyan Ibn Uyaynah, Imam Abu Hanifa, Imam Malik,n.k. Na kisha baada yao kinafuata kizazi cha Wanazuoni waliosomeshwa na Wanafunzi wa Tabii Tabiin na ndani yake mna kina Imam Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, n.k.na Wanazuoni wa kizazi baada ya kizazi hadi kufikia kwetu sisi.

Hivyo Miongoni mwa Hadith zinazoonesha kuhusiana na changamoto zinazotokea katika Ibada ya Sala hususan katika hatua ya Sijda na namna ya kukabiliana nazo bila ya Kuharibu Sala yako basi ni ile isemayo:

حَدَّثَنَا مُوسَى، قَالَ حَدَّثَنَا هَمَّامٌ، عَنْ يَحْيَى، عَنْ أَبِي سَلَمَةَ، قَالَ انْطَلَقْتُ إِلَى أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ فَقُلْتُ أَلاَ تَخْرُجُ بِنَا إِلَى النَّخْلِ نَتَحَدَّثْ فَخَرَجَ. فَقَالَ قُلْتُ حَدِّثْنِي مَا، سَمِعْتَ مِنَ النَّبِيِّ ﷺ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ. قَالَ اعْتَكَفَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ عَشْرَ الأُوَلِ مِنْ رَمَضَانَ، وَاعْتَكَفْنَا مَعَهُ، فَأَتَاهُ جِبْرِيلُ فَقَالَ إِنَّ الَّذِي تَطْلُبُ أَمَامَكَ. فَاعْتَكَفَ الْعَشْرَ الأَوْسَطَ، فَاعْتَكَفْنَا مَعَهُ، فَأَتَاهُ جِبْرِيلُ فَقَالَ إِنَّ الَّذِي تَطْلُبُ أَمَامَكَ. فَقَامَ النَّبِيُّ ﷺ خَطِيبًا صَبِيحَةَ عِشْرِينَ مِنْ رَمَضَانَ فَقَالَ " مَنْ كَانَ اعْتَكَفَ مَعَ النَّبِيِّ ﷺ فَلْيَرْجِعْ، فَإِنِّي أُرِيتُ لَيْلَةَ الْقَدْرِ، وَإِنِّي نُسِّيتُهَا، وَإِنَّهَا فِي الْعَشْرِ الأَوَاخِرِ فِي وِتْرٍ، وَإِنِّي رَأَيْتُ كَأَنِّي أَسْجُدُ فِي طِينٍ وَمَاءٍ ". وَكَانَ سَقْفُ الْمَسْجِدِ جَرِيدَ النَّخْلِ وَمَا نَرَى فِي السَّمَاءِ شَيْئًا، فَجَاءَتْ قَزْعَةٌ فَأُمْطِرْنَا، فَصَلَّى بِنَا النَّبِيُّ ﷺ حَتَّى رَأَيْتُ أَثَرَ الطِّينِ وَالْمَاءِ عَلَى جَبْهَةِ رَسُولِ اللَّهِ ﷺ وَأَرْنَبَتِهِ تَصْدِيقَ رُؤْيَاهُ

Amesema Musa kua amesema Hamam kua amesema Yahya, kua amesema Abu Salama kua: '**Siku moja mimi nilienda kwa Abu Said Al Khudri *(Radhi Allahu Anhu)* na kumwambia: 'Vipi Ewe Abu Khudhri, Hivi Jee unaweza kuja kwenye Mitende ili tupate kuzungumza kidogo?'**

Hivyo Abu Said Al Khudhri *(Radhi Allahu Anhu)* akatoka nami na nikamwambia: 'Hebu Niambie kuhusiana na Laylat Al Qadr'

Abu Said Al Khudhr*(Radhi Allahu Anhu)* akasema: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikaa Itiqaf katika Siku 10 za Mwanzoni za mwezi wa Ramadhani, nasi tukakaa pamoja nae. Hivyo Akaja Malaika Jibril na Kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Usiku unaoutafuta Uko Mbele yako.''

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakaa Itiqaf katika Siku 10 za Pili za mwezi wa Ramadhani, nasi tukakaa pamoja nae. Hivyo Akaja Malaika Jibril na Kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Usiku unaoutafuta Uko Mbele yako.'

Hivyo katika Asubuhi ya siku ya mwezi 20 *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatoa Khutba na kusema: 'Yeyote yule anaetaka kuendelea Kukaa Itiqaf pamoja nami nasi na akae kwani nimeoneshwa Usiku wa Laylat Al Qadr, lakini nimeisahau Tarehe yakeLakini ndani ya Ndoto hio nimejiona nikiwa nimesujudu ndani ya Tope na Maji.'

Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua: 'Katika wakati huo Msikiti ulikua umeezekwa kwa Makuti ya Mtende, na katika kipindi hicho (Cha Ramadhani hio) Mbingu zilikua Safi kabisa hakuna Wingu hata Moja Lakini (Usiku wake siku hio) kikatokea Kiwingu na Mvua ikanyesha (Alfajir wakati) *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akitusalisha. Nami Nikaona Alama za Tope kwenye Paji lake la Uso na kwenye Pua ya*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na Hivyo hii ikawa ndio Thibitisho la Ndoto aliyoota *(Sahih Bukhari na Muslim)*

Naam..ingawa hii ni Hadith ya Laylat Al Qadr na Wanazuoni wanasema kua ilikua ni Usiku wa Kuamkia Mwezi 21 Ramadhan lakini ndani yake inatuonesha mambo Muhimu kuhusiana na Sala hii ambayo ilikua ni ya Alfajir na Mazingira yake ilivyokua.

Kwani Hadith hii kwanza inatuonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum*walikua Wakisali kwenye Msitiki ambao Ulikua Unavuja, kisha ulikua hauna Sakafu ndani yake, bali kuna mchanga Mtupu yaani sawasawa na kusali nje na hivyo Mvua iliponyesha basi Maji yaliingia Ndani kiasi ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* wakajikuta wamo kwenye Tope.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaongoza Sala huku akiwa anasujudu Ndani ya Tope kama alivyooneshwa kwenye Ndoto. Ambapo hii inaonesha kua mbali ya Ugumu wa Mazingira waliyokua nayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum*, lakini Sala iliendelea na Sijda ilitekelezwa Ipasavyo.

Na pia hadith inatuonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliposujudu aligusisha Ardhini Paji lake la Uso na Pua yake pia, kiasi ya kua Viungo hivyo vilijaa Tope.

Na Miongoni pia mwa Hadith zinazoonesha kuhusiana na changamoto zinazotokea katika Ibada ya Sala na kukabliana basi ni ile hadithi iliyonukuliwa na Imam Ahmad Ibn Hanbal katika Musnad yake ambayo inasema**: 'Amesema Jabir Ibn Abd Allah Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Mimi nilikua pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* ambapo uliingia wakati wa Sala ya Adhuhuri, hivyo**

nikachukua Gao la Kokoto kutokana na Hali ya Joto kali, basi nikaziweka kwenye mkono wangu mmoja na kisha kuziweka kwenye Mkono mwengine ili kuzifanya zipoe, na kisha nikaziweka chini kwa ajili ya Kusjudia Juu yake.''*(Musnad Imam Ahmad)*

Naam..hii hadith inatuonesha namna Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walivyokua wakipata tabu katika ufanyaji wa Ibada zao kutokana na hali ya Mazingira waliyokua wakiishi. Jangwani hakuna Mafeni wala Paa hivyo Jua likipiga basi Ardhi hua inaunguza sana kiasi ya kua inakua Vigumu kusujudu juu yake.

Kama vile ambapo inathibitishwa na Zayd Ibn Thabit *Radhi Allahu Anhu* plae aliposema kua: **'Hakuna Sala iliyokua Ngumu kwetu sisi kama Sala ya Adhuhuri, lakini hata hivyo kamwe hatukua ni wenye kuachana nayo.'***(Sunnan Abu Daud)*

Na akasema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: *'**Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam*** **alikua akisali huku amevaa Nguo Moja huku akiwa amefunika Uso wake kwa sehemu ya Nguo hio kwa ajili ya Kujilinda na Umoto au Ubaridi wa Ardh**i.' *(Musnad Imam Ahmad)*

Na anasema Khabbab Ibm Arat *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Sisi tulilalamika kwa *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Ukali wa Joto la Ardhini ambalo lilikua linatuumiza kwenye Paji la Uso na Viganja vyetu lakini hakusema kitu.'***(Imam Al Bayhaqi)*

Hivyo ingawa kuna Hadith kadhaa zilisema kuhusiana na Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na *RasulAllah Salallahu Alayhi wa Salam* mwenyewe kua waliweka Vilemba chini Kwa ajili ya Kusujudia lakini bado Wanazuoni wanarudi kwenye Hadith ya Kuu ya Msingi na ya mwanzo inayozungumzia Masharti ya Kusujudia Viungo 7 vya Mwili. Ambapo na hii pia ni Kulingana na Hadith ya Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu*inayozungumzia Usiku wa Laylat Al Qadr tuliyoiona ambayo iliyoonesha Kujaa Tope kwa Paji la Uso na Pua ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama alivyooneshwa katika Ndoto. Na Kisha pia uthibitisho wa Hadith hii ya Khabbab *Radhi Allahu Anhu*.

Na hivyo basi Wanazuoni wanakubaliana kua: **'Hua ni Bora kwa Mtu Mwenye Kusali kugusisha Paji la Uso na Pua Ardhini, isipokua pale itakapokua kuna Dharura basi ndio unaweza kutandika kitu Juu ya Ardhi.'**

Na Abū Isḥāq Ibrāhīm Ibn ʿAlī Al Shīrāzī Al Hamdani Al Hamawi Al Shafii anasema kua: **'Amesema Imam Al Shafii amesema kua Paji la Uso linatakiwa lisifunikwe, na pia amesema katika sehemu nyengine kua 'Paji la Uso ni Wajib kua wazi, na kama Mtu ataweka Mkono chini na kisha kusujudu Juu yake basi Sijda hio hua ni Batili.'**

Kwani anasema Imam Al Allamah Al Muhadith Al Adib Abu Hasan Ali Izza Ad Din Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Athir Al Jazari Al Shafii kuhusiana na Hadith ya Khabbab kua: **'Kwa kua Masahaba Walilalamika kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Joto la Ardhini linalounguza, Na *Rasul Allah Salallabu Alayhi wa Salam* hakuwaambia Wasujudu Juu ya Nguo Mbali ya kua ni Mwenye Kua na Huruma kwa Waumini, lakini aliwawajibisha kuweka Mapaji yao ya Uso Ardhini**.'

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: **Wanazuoni Wanakubaliana kua bila kutofautiana kua Inapendekezwa kwa Paji la Uso na Pua kugusa Ardhini moja kwa Moja katika Wakati wa Kusjudu**. **Na katika Madhhab yetu ya Imam Al Shafii basi ni kua; Yeyote yule Atakaesujudu Juu ya Mkono wake, Au Juu ya Mkunjo waWa Kilemba chake, Au Juu ya Mkono wa Nguo Yake aliyoivaa, au Mwishoni mwa Kilemba**

chake na vitu vyote vinavyoenda nae kwa kujitegemea katika hatua zake za Sala anapokaa na Kunyanyuka basi Sala yake ni Batili.*'(Al Majmuu)*

Na Anasema *Al Muhaqqiq* Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: '**Uthibitisho wa Madhhab yetu ni Hadith ya Khabbab Ibn Arat pale aliposema kua: 'Tulilalamika sisi kwa *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Kuunguza kwa Ardhi Kwenye Paji la Uso na Viganja Lakini Hakutukubalia Hivyo kama ingekua Haitakiwi Kuviwacha Wazi basi angewaambia Wavifunike.''***(Tuhfa)***

Na kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Abd Rahman Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Hakuna Ulazima kwa Mtu anaesali Kugusisha sehemu yake yeyote ya mwili moja kwa Moja juu ya Ardhi, na Qadhi Iyad amesema kua: 'Kama Mtu atasujudu Juu ya Kilemba chake, au Juu ya Mkono wa Nguo yake basi Sala yake hua ni Sahih kulingana na Moja kati ya Hadith ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Malik na Imam Abu Hanifa pia.''**

Ambapo Mtizamo huu pia ni wa Imam Ataa Ibn Rabah, Imam Tawis, Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Abd Rahmani Ash Shabi, Imam Al Awzai, Imam Muhammad Ibn Is-haq n.k. Na Wanaosema kua Inaruhusika Kusjudu Mwishoni mwa Kilemba, Kofia au Hijab aliyokivaa Mtu ni Imam AlQadhi Al Shurayh Al Yaman Imam Hasan Al Basr, Imam Al Makhul, Imam Abd Rahman Ibn Yazid n.k

SUJUD –MASHARTI 7 YA KUSUJUDU

❖❖❖

Ama kuhusiana na Mashartiya Sujud basi anasema Al Alamah, Al Faqih Al Sayid Al Imam Ahmad Ibn Umar Al Shatiri Al Alawi At Tarimi Al Shafii kua:

Ili Sujudu Ya Sala iwe ni Yenye Kukamilika basi Inabidi Itimize Masharti 7 Yafuatayo:

1- **Isujudiwekwa Kutumia Viungo 7 vya Mwili kama ilivyosema Hadith.**
2- **Paji La Uso Liwe Liko Wazi yaani Halikuzibwa.**
3- **Kuugusisha Kichwa na Paji la Uso Ardhini katika sehemu ya Kusujudia kwa Kuuhisi wa Shingo na Mwili kwenye Paji la Uso juu ya Ardhi.**
4- **Kusujudu huko kuwe kwa nia ya Kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu.**
5- **Kutosujudia Juu ya Kitu ambacho Kitakua kina Kinatembea na wewe Katika Vitendo vyako vya Ndani ya Sala.**
6- **Mgongo na Makalio yawe Juu zaidi kiusawa kulingana na Kichwa, yaani Kichwa kiwe Chini zaidi.**
7- **Upatikane Utulivu ndani ya Kitendo cha Kusujudu.***(Nayl Al Rajaa Bi Sharh Safinat Al Najah)*

Hivyo haya ndio Masharti ya Sujud Kulingana na Mtizamo wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii.

Ambapo amesema Sultan Al Ulamaa, Shaykh Ul Islami Al Imam Abu Muhammad Izza Ad Din Abd Al Aziz Ibn Abd Salam Ibn Abi Qasim Ibn Hasan Al Sulami Al Shafii kua: **'Hua ni Sunnah kufumbua**

macho kwa mtu mwenye kusjudu'. Ambapo Mtizamo huo pi aunaungwa mkono naShaykh Ul Islami Imam Abu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Bahadir Al Zarkashi Al Shafi

Na Tunakumbushana kwa sababu katika Kuangalia kuhusiana na Sujud basi tumeona kua baadhi ya wakati hua kuna Changamoto. Ambazo kama tulivyoziona kwenye Hadith kuhusiana na utaratibu wa Kusujudu kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kulingana na Mazingira Tofauti, ikiwemo hali ya Jua kali, hali ya Mvua, hali ya kuwepo kwa Tope na kuwepo kwa Baridi pia katika sehemu ya Kusujudia.

Lakini hata hivyokuna baadhi ya Mifano hatujaiangalia ambayo inaweza kututokea mimi na wewe katika Mazingira yetu. Kwa mfano: '**Tumefika Msikitini au katika Eneo la Kusalia na kisha baada ya Kuingia ndani ya Sala tukagundua kua katika wakati wa Kusujudu Mtu anahisi Maumivu Makali sana kwenye Paji la Uso na Pua yake kutokana na Sehemu anayosujudia labdaKuna Vigae vidogo vidogo ambavyo haikuwezekana kuonekana kwa Macho hapo KablaAu Labda Kuna Mawe, Au Miba au Siafu, au kitu ambacho kinaweza kusababisha Madhara kwa anaesali**. **Hivyo Jee katika Hali kama hii Tunatakiwa Kufanya Nini? Wakati Tayari tumeshaingia ndani ya Sala?.'**

Hivyo Ili tuweze kujua nini cha Kufanya basi ndio imebidi Tumtafute Imam Ahmad Ibn Umar Al Shatiri ili atufahamishe kuhusiana na Masharti ya Kusujudu ndani ya Sala. Na kama tunavyoona katika Masharti basi tunaona kua katika Mazingira kama haya basi Mtu anaweza kutekeleza Masharti yote haya kwa ukamilifu lakini atashindwa kutekeleza Sharti la Mwisho kutokana na Maumivu yatakayompelekea Kukosa Utulivu, kwani Chini Hapasujudiki Ipasavyo.

Hivyo Wanazuoni wanasema kuhusiana na inapotokea hali kama hii basi Hukmu yake hua ni kama Ifuatavyo:

1-Kama Mtu atakua Ndio kwanza Ameingia kwenye sujudu Juu ya Ardhi husika. **Na hivyo Hajawahi kupata Utulivu akahisi Maumivu yenye kutaka kumsababishia Madhara basi .Mtu husika anaruhusika hapo hapo Kunyanyua Kichwa na Kusjudu Sehemu nyengine isiyokua na Madhara kwake, na Sala yake itakua iko Sahih.**

2-Kama Mtu atakua Ameshaingia kwenye Sujudu na amekaa na kupata Utulivu na kisha akaanza kuhisi Maumivu, basi Mtu huyo anaruhuisika Kunyanyua Kichwa chake. **Na kusujujudia Sehemu Nyengine, Lakini hata hivyo Sala yake Itakua ni yenye Kubatilika na hivyo Itambidi Kuirudia Sala yake hio.**

3-Kama Mtu atakua Ameshaingia kwenye Sujudu na amekaa na kupata Utulivu na kisha akaanza kuhisi Maumivu, basi Mtu huyo anaruhuisika Kukiondoa Kichwa chake kutoka katika Sehemu na kuendelea na Sujud hio pembeni yak lakini bila ya Kukinyanyua Kichwa chake, na kufanya hivyo hakutopelekea kubatilika kwa Sala yake.

Kwani anasema Anwar Al Azhar Al Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Khatib Al Shhirbini kua: '**Mtu anaesali Anaweza Kunyanyua Paji lake la Uso Kutoka Katika Sijda yake kabla ya kuupata Utulivu wa Ndani ya Sijda hio kutokana na Khofu ya Kitu lakini Asinyanyue Kichwa kwa Nia ya Kua Kufanya kwake huko ni Kunakotokana na Khofu, kwani akikinyanyua Kutokana na Khofu ya Kitu basi hua si Sababu inayokubalika kunyanyua Kichwa kutoka kwenye Sijda na hivyo Itambidi Mtu huyo arudishe Kichwa chini kwenye Sijda.'***(Al Iqna Fii Hal Al Faath Abi Shujaa)*

Nakabla ya kuendelea basi inabidi tukumbushane kua tunapozungumzia kuhusiana na Mda wa Kupata Utulivu Ndani ya Sijda basi hua tunazungumzia Mda wa Kufanya Dhikr Allah Ndani yake.

Ambapo anasema Imam Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Ahmad Al Bajuri Al Shafii kua: '**Sujud Lazima Itekelezwe kwa Kutumia Viungo vyote 7 vya Kusujudia katika Utulivu wake**. **Ambapo Sehemu Muhimu kabisa hua ni Paji la Uso, na Ndio Maana Paji la Uso lililozibwa au Kufunikwa Hua Sijda yake ni Batili. Na Hivyo pia Mtu yeyote atakaenyanyua Kichwa chake kutoka kwenye Sijda Bila ya Sababu basi pia Sijda yake hua ni Batil**i'*(Hashiyyah Al Bajuri)*

Kwani Kisharia basi Kunyanyua Kwa mtu Kichwa chake kutoka kwenye Sijida hua kuna hesabiaa katika Hali mbili zifuatazo:

1-Kunyanyua Kichwa kutoka katika Sijda Kusikoruhusika Kisharia ambako huipelekea Sijda Husika kua Batili na hivyo Hata Sala yenyewe pia hua ni Batili.

2-Kunyanyua Kichwa Kutoka katika Sijda kunakotokana na Sababu Inayokubalika Kisharia ambako kumegawika katika Hali Mbili zifuatazo:

-Kwanza hua inakubalika Kisharia Kunyanyua Kichwa pale Mtu atakapokua Amesujudu juu ya Kitu Chenye ncha au Kitu chochote kitakachomsababishia madhara kwa Paji lake La Uso, ambapo katika hali ya mazingira kama Haya basi Mtu anaruhusika Kunyanyua Kichwa chake lakini kwa sharti la kua alikua bado hajaingia katika Hali ya Kupata Utulivu ndani ya Sijda.

-Pili, kama Ikiwa Mtu amehisi Maumivu hayo katika wakati ambao Tayari ameshaingia katika hali ya Kupata Utulivu na hapo hapo akanyanyua kichwa kwa sababu ya Maumivu basi Sijda yake hua Batili'*(Hashiyyah Al Bajuri)*

Am kwa Upande mwengine basi inasema Kamusi Fiqh ya Kiislam ya Kuwait yenye kujumuisha Mitizamo ya Fiqh za Madhhab ya Kiislam kua: '**Kama ikiwa Mtu atanyanyua Kichwa chake kutoka kwenye Sijda kwa Sababu ya kua ameogopa Kitu fulani, basi Khofu hio hua si sababu inayotomsheleza mtu na haimruhusu Mtu kunyangua Kichwa chake kutoka kwenye Sujud, na Hivyo hapo hapo anatakiwa arudishe Kichwa chake kwenye Sujud.'**

'Na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wanasema kua: Ni Sharti la Kurukuu na Kusujudu na kutoka Ndani ya Rukuu na Sujudu kua Kufanya hivyo kuwe ni Kutokana na Kumuabudia *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Hivyo Mtu akiingia na Kutoka kwenye Rukuu na Sujudu kutokana na Khofu ya Kitu chengine basi hua Haitoshelezi, kufanya hivyo kwani Nia Ya Kurukuu na Kusjudu ni kwa Ajili ya Kusali.'*(Mawsuat Islamaiyyat Fiqhiyat Quwaitiya)*

Naam..hivyo anasema Imam Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Ahmad Al Bajuri Al Shafii kua: '**Kama ikiwa Mtu atasjudu katika sehemu ambayo itakua inamuumiza Kwenye Paji lake la Uso kwa mfano, na kisha akakiondoa Kichwa chake kutoka katika sehemu hio bila ya kukinyanyua kutoka juu ya Ardhi ya sehemu hio anayosujudiaBasi Sala ya Mtu huyo hua si yenye kuathirika**.

Na kama atakiondoa Kichwa hicho Kabla ya Kupata Utulivu ndani yake katika Sijida hio kutoka katika Sehemu hio anayosujudia ksa kukinyanyua Kichwa na kikaaa ni chenye kuachana na Ardhi kwa kutoigusa katika kuondolewa kwake basi pia hii hua haiiathiri Sala yake. Lakini kama ikiwa alifanya hivyo yaani kukiondoa kichwa kutoka Juu ya Ardhi kwa kukinyanyua kutokana na kuhisi maumivu baada ya kua tayari ameshaingia kwenye hali ya Utulivu wa Sijda husika basi hapa Mtu husika atakua ni mwenye Kuiathiri Sala yake na kuidhuru kwani atakua ameongeza

Sijda Nyengine ndani ya Sijda ya Sala yake na Sala inabatilika Na pia kama atakinyanyua Kichwa kutoka kwenye Sijda bila ya sababu yeyote inayoruhusika Kishariah basi Sala yake pia itakua Imebatilika'*(Hashiyyah Al Baijuri)*

Na anasema Imam Daud Abd Allah Ibn Idris Al Fatani Al Shafii kua: '**Kama Mtu atasujudu kwenye sehemu inayomuumiza na hivyo atanyanyua Kichwa chake na kisha akasjudu tena katika sehemu nyengine, basi Sala yake Mtu huyo itabatilika**. **Kama ikiwa Sujud hio imewahi kupata Utulivu wa Mwanzoni,lakini kama ikiwa hakuwahi kuupata Utulivu wa Mwanzoni mwa Sijda basi Kitendo hicho kitahesabika kua ni kitendo kidogo kisichoweza kuhesabika**. **Hivyo basi Mtu Anatakiwa kutonyanyua Kichwa chake, bali anatakiwa akisogeze taratibu bila kukinyanyua kutoka kwenye Sehemu inahomuumiza ili asiwe ni mwenye Kubatilisha Sala yak**e'*(Bughyah Al Tulab)*

Hivyo ndivyo inavyotakiwa kufanya pale unapotokezewa na hali kama hii ya dharura ndani ya Sala katika Wakati wa Kusujudu.Na tunakumbushana hivi kwa sababu Mtu unaweza kusali katika sehemu yeyote Juu ya Ardhi kama zilivyosema Hadith zifuatazo:

عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْأَرْضُ كُلُّهَا مَسْجِدٌ إِلَّا الْمَقْبَرَةَ وَالْحَمَّامَ

Amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua **: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ardhi nzima imejaaliwa kua ni Sehemu ya Kusalia isipokua Makaburini na Vyooni.'***(Imam At Tirmidhii)***

Na amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua:

قال رسول الله ﷺ : (أعطيت خمسا، لم يعطهن أحد من الأنبياء قبلي: نصرت بالرعب مسيرة شهر، وجعلت لي الأرض مسجدا وطهورا، وأيما رجل من أمتي أدركته الصلاة فليصل، وأحلت لي الغنائم، وكان النبي يبعث إلى قومه خاصة، وبعثت إلى الناس كافة، وأعطيت الشفاعة)

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua;'Hakika Mimi nimepewa Mambo matano ambayo hakupewa Nabii yeyote Kabla yangu:Nimepewa Ushindi Dhidi ya Khofu kwa Umbali wa Masafa ya Safari ya Mwezi mmoja: Na Ardhi imefanywa kua ni Sehemu ya Kusalia na Kujitoharishia kwa ajili yangu. **Na Hivyo Mtu yeyote kutoka katika Ummah wangu niliemuamrisha Kusali basi na Asali(Juu yake); Na Ngawira imehalalishwa kwa ajili yangu, na Mitume walitumwa kwa watu wao lakini mimi nimetumwa kwa Watu wote'***(Sahih Bukhari)***

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Ardhi yote imejaaliwa kua ni sehemu ya Kusalia na kujitoharishia Kwa Ajili yangu mimi na kwa ajili ya Ummah wangu; Hivyo popote pale utakapomfikia mtu wa Ummah wangu wakati wa kusali, basi atakua na sehemu ya kusalia na kujitoharishia pembeni yakeKwani wale waliotangulia kabla yangu walidhania kua hii imezidi tena, na hivyo walikua wakisali Makanisani na katika Masinagogi tu'***(Sahih Hadith kutoka kwa Imam Al Bayhaqi na Imam Ahmad)***

SUJUD KATIKA KANISA, HEKALUNI, MAZIZINI, NJIANI N.K.

❖❖❖

Kama tulivyoona katika Hadith ya Imam Al Tirmidhii ambayo imesema kua:

عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ الْأَرْضُ كُلُّهَا مَسْجِدٌ إِلَّا الْمَقْبَرَةَ وَالْحَمَّامَ

‘**Amesema Abu Said Al Khudhry*Radhi Allahu Anhu* kua:Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ardhi nzima imejaaliwa kua ni Sehemu ya KusaliaIsipokua Makaburini na Vyooni’***(Imam At Tirmidhii)***

Ingawa Hadith imezungumzia kuhusiana na Kusali katika sehemu yeyote na hivyo kuruhusu Kusjudia Ardhi ya sehemu yeyote isipokua Chooni na Makaburini, Lakini hata hivyo kuna sehemu za Ardhi ambazo Wanazuoni wametofautiana Juu yake Kusjudia, kwa Mfano kwenye Makanisa na Mahekalu au Masinagogi.

Lakini kwa Upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: ‘**Hairuhusiwi Kusali ndani ya Makanisa, Mahekalu au Masinagogi ikiwa ndani ya kuna Masanamu.’**

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: ‘**Haipendekezwi na ni Makruh Kuingia au Kusali ndani ya Makanisa, Masinagogi au Mahekalu iwe kuna Masanamu, ama Picha Ama la.Na hii ni kwa Sababu Sehemu hizo ni sehemu ambazo ndani yake Mnaabudiwa Asiekua *Allah Subhanah wa Ta'al****a****’***(Nihayat Al Muhtaj, Radd Al Mukhtar)*

Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Maliki wamesema: ‘**Haipendezi Kusali katika Hekalu au Kanisa ambalo halikaliwi na wala halina picha ndani yake, na humo ndani na hakuna Wakristo au Mayahudi wanaosali ndani ya Kanisa Hekalu, yaani ikiwa Muislamu atapata Kanisa au Hekalu lisilotumiwa na watu na bila ya kua na uchafu au picha ndani yake, katika hali ya mazingira ambayo hakuna sehemu Nyengine ya Kusali ndani yake, basi hua inaruhusika kwake Kusali ndani yao. Kwani katika wakati wa Kipindi cha mamlaka ya Umar Ibn Abd Al Azizi, ilitokea walikua safarini na ikawa hakuna sehemu ambayo ni safi zaidi au bora kuliko bay'ah - yaani, kwenye Hekalu –Hivyo basi Umar Ibn Abd Al Azizakaamrisha lisafishwe na kisha Wakasali ndani yake.**

Na kwa upande mwengine basi pia kuna Mtizamo usemao kua **Hairuhusiki kwa Muislam kuingia kwenye sehemu za Kuabudia za Dini nyengine isipokua pale watakapokua wameruhusiwa na wenye Sehemu hio, na kuna Wanazuoni wa Madhhab ya Imam al Shafii wasemao pia kua Inaruhusika kuingia katika Sehemu hizo hata bila ya Ruhusa zao.’** *(Al Mawsuat Fiqhiyat Kuwaitiyah)*

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Muhammad Ibn Tamim Al Harani Al Hanbali basi anasema kua: ‘**Inaruhusika kuingia kwenye Makanisa na Mahekalu na Kusali ndani yake kama ikiaa hakuna Masanamu na picha Ndani yake.’**

Na akasema Imam Abu Al Wafaa Ali Ibn Aqiil Ibn Ahmad Al Baghdadi Al Hanbali kua: ‘**Ni Makruh kuingia katika sehemu hizo kwa sababu ya Masanamu na Picha zilizomo ndani yake.’**

Ambapo kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Abd Rahman Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye anasema kua:

فَصْلٌ: وَلَا بَأْسَ بِالصَّلَاةِ فِي الْكَنِيسَةِ النَّظِيفَةِ، رَخَّصَ فِيهَا الْحَسَنُ وَعُمَرُ بْنُ عَبْدِ الْعَزِيزِ وَالشَّعْبِيُّ وَالْأَوْزَاعِيُّ وَسَعِيدُ بْنُ عَبْدِ الْعَزِيزِ (٩٦٩) وَرُوِيَ أَيْضًا عَنْ عُمَرَ وَأَبِي مُوسَى، وَكَرِهَ ابْنُ عَبَّاسٍ وَمَالِكٌ الْكَنَائِسَ؛ مِنْ أَجْلِ الصُّوَرِ. وَلَنَا «، أَنَّ النَّبِيَّ — صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ — صَلَّى فِي الْكَعْبَةِ وَفِيهَا «صُوَرٌ» ، ثُمَّ هِيَ دَاخِلَةٌ فِي قَوْلِهِ — عَلَيْهِ السَّلَامُ -: «فَأَيْنَمَا أَدْرَكَتْكَ الصَّلَاةُ فَصَلِّ، فَإِنَّهُ مَسْجِدٌ

‘Wala hakuna Tatizo Kusali katika Knaisa lililosafiKulingana na Mtizamo wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu,* Hasan Al Basr, Umar Ibn Abd Al Aziz, Al Shabi, Al Awzai na Said Ibn Abd Al Azizi basi wao wanasema kua Inaruhusika Kusali ndani ya Kanisa lililokua Safi.Ama Kulingana na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na Imam Malik basi hua ni Makruh kwa sababu ya Masanamu na Picha zilizomo ndani yake.’

‘Lakini hata hivyo basi hua Inafaa kusali ndani yake kwasababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali ndani ya Al Kaabah katika wakati ambao Mlikua na Picha ndani yake, na hii pia ni kutokana na kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo:Unapowadia Wakati wa Sala basi Salini Mahali popote kwani mahali popote hua ni Masjid.’ *(Sahih Muslim)*

Imam Ibn Qudamah anaendelea kusema kua:

وَرَوَى ابْنُ عَائِذٍ فِي ’’ فُتُوحِ الشَّامِ ‘‘، أَنَّ النَّصَارَى صَنَعُوا لِعُمَرَ — رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ -، حِينَ قَدِمَ الشَّامَ، طَعَامًا، فَدَعَوْهُ، فَقَالَ: أَيْنَ هُوَ؟ قَالُوا: فِي الْكَنِيسَةِ، فَأَبَى أَنْ يَذْهَبَ، وَقَالَ لِعَلِيٍّ: امْضِ بِالنَّاسِ، فَلْيَتَغَدَّوْا. فَذَهَبَ عَلِيٌّ — رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ — بِالنَّاسِ، فَدَخَلَ الْكَنِيسَةَ، وَتَغَدَّى هُوَ وَالْمُسْلِمُونَ، وَجَعَلَ عَلِيٌّ يَنْظُرُ إلَى الصُّوَرِ، وَقَالَ: مَا عَلَى أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ لَوْ دَخَلَ فَأَكَلَ، وَهَذَا اتِّفَاقٌ مِنْهُمْ عَلَى إبَاحَةِ دُخُولِهَا وَفِيهَا الصُّوَرُ، وَلِأَنَّ دُخُولَ الْكَنَائِسِ وَالْبِيَعِ غَيْرُ مُحَرَّمٍ

‘Na amepokea Ibn Aidhin katika (Fat-h Sham) Ufunguzi wa Sham kua:Wakati Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alipoiteka Ardhi ya Sham ambyo mwanzoni ilikua chini ya Wakristo, basi alialikwa Chakula na Wakrksto hao ambacho Kiliandaliwa Kanisani. Lakini hata hivyo Umar Ibn Al Khattab*Radhi Allahu Anhu* alikataa Mualiko huo na Badala yake akamwambia Ali Ibn Abi *Talib Radhi Allahu Anhu* achukue nafasi yake hio ya Mualiko. Na Ali Ibn Abi Talib*Radhi Allahu Anhu* akaenda Kanisani na Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na akaziangalia Picha zilizomo ndani yake na kusema; ‘Sijui ana nini Amir Al Muuminina’Na kisha akala’’

Na hivyo hii inaaonesha kua Masahaba *Radhi Allahu Anhu* walikua wamekubaliana kua kuingia Makanisani na kwenye Masinagogi hakujakatazwa.’ *(Al Mughni)*

Inawekana ikawa kuna watu wakajiuliza kwanini Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*akakataa Mualiko huo na akamtuma Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* badala yake? ambapo tunapofutilia

zaidi basi tunaona kua Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*hakutaka kuhudhuria Mualiko huo kwa sababu alikua ana khofu kua huenda akikubalia basi baadae Waislam wangefuata Mfano wake na kuyachukua Makanisa na kuyataifisha na kuyageuza kua Misikiti baada yake, kwani Mtizamo wa maneno haya aliudhihirisha pale aliouteka Mji wa Jerusalem nahivyo ulipowadia mda wa kusali basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*alikataa kusali ndani ya Kanisa la Jerusalem na hivyo akasali nje yake badala yake.

Ambapo kwa Upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi basi yeye anasema kuhusiana na Kusujudu na Kusali katika sehemu kama hizo yaani Makanisani, Masinagogi,Mahekalu n.k kua: '**Ni Makruh Kusali katika Viota vya Shaytani, ambazo ni sehemu za Pombe, Uongo na kila aina ya Dhambi**'*(Al Majmuu)*

Hivyo Kusali au Kusujudia katika sehemu kama hizo Hua hakuifanyi Sala husika Kua Batili bali hua inakirihisha hususan pale inapokua kuna Masanam na Picha ndani yake, ila inapokua kuna Dharura labda kwa mfano katika Mji husika kumetokea Maafa ya Mafuriko na hakuna sehemu isiyokua na Maji isipokua Kanisani basi hua inaruhusika kusjudu na Kusali ndani yake lakini inabidi Masanam na picha zifunikwe ili zisionekane, kwani kuonekana kwake hukuondolea Umakini wa Ibada kutokana na kua ni Maksri ya Shaytani.

Kwaupande mwengine basi mbali ya Hadith ya Abu Said Al Khudri *Radhi Allahu Anhu*kua ni Hadith yenye Kukataza sehemu mbili zisizofaa Kusujudia ambazo ni Vyooni na Makaburini lakini pia kuna Hadith isemayo:

حَدَّثَنَا عُثْمَانُ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، حَدَّثَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، حَدَّثَنَا الأَعْمَشُ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ الرَّازِيِّ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبِي لَيْلَى، عَنِ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ، قَالَ سُئِلَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَنِ الْوُضُوءِ مِنْ لُحُومِ الإِبِلِ فَقَالَ " تَوَضَّئُوا مِنْهَا " . وَسُئِلَ عَنْ لُحُومِ الْغَنَمِ فَقَالَ " لاَ تَتَوَضَّئُوا مِنْهَا " . وَسُئِلَ عَنِ الصَّلاَةِ فِي مَبَارِكِ الإِبِلِ فَقَالَ " لاَ تُصَلُّوا فِي مَبَارِكِ الإِبِلِ فَإِنَّهَا مِنَ الشَّيَاطِينِ " . وَسُئِلَ عَنِ الصَّلاَةِ فِي مَرَابِضِ الْغَنَمِ فَقَالَ " صَلُّوا فِيهَا فَإِنَّهَا بَرَكَةٌ

Amesema Uthman Ibn Abi Shaybah kua amesema Abu Muawwiyah, kua amesema Imam Al Amash kua amesema Imam Abd Allahi Ibn Abd Allahi Al Razi kua amesema Abd Rahman Ibn Abi Layla, kua Amesema Al Baraa Ibn A'zib *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa Kuhusiana na Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia, ambapo nae akajibu kwa kusema: 'Tia Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia.'

Akaulizwa kuhusiana na Kutia Udhu baada ya Kula Nyama (Nyenginezo zilizoruhusiwa kula). Ambapo akasema 'Haina Haja ya Kutia Udhu baada ya Kula Nyama.'

Akaulizwa kuhusiana na Kusali katika sehemu ambazo wanalala Ngamia, ambapo nae akajibu: 'Haifai Kusali katika Sehemu ambazo Ngamia hua wanalala, kwani hizo ni sehemu za Shaytani.'

Akaulizwa Kuhusiana na Kusali katika Sehemu Wanazolala Kondoo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Mnaweza Kusali katika sehemu kama hizo kwani ni sehemu zenye Baraka.'(*Sahih Muslim, Sunan Imam Abu Daud)*

Naam hii ni Hadith ambayo imetaja miongoni mwa sehemu Ambazo Imekatazwa Kusujudu ambayo ni katika Sehemu za Ardhi wanazolala na Kupumzika Ngamia yaani kwenye Zizi lao, Banda lao nk. Na hii ni kwa sababu sehemu hizo hua zinapendwa na Shaytani, na Hivyo kama Mtu akisali ndani yake sehemu hizo basi atakosa Umakini na Utulivu ndani ya Sala yake, Kwani huenda Ngamia huyo akakupiga Teke, na hivyo kutokana na kua ni sehemu zenye kupelekea kukosekana kwa Umakini na Utulivu ambavyo ni vitu Muhimu katika Sala basi ndio *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akakataza.

Na pia kuna Hadith nyengine inayoainisha sehemu 7 ambazo zimekatazwa Kusujudia Kutoka kwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:

ابْنِ عُمَرَ –رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا– قَالَ: نَهَى النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم أَنْ يُصَلَّى فِي سَبْعِ مَوَاطِنَ: الْمَزْبَلَةِ، وَالْمَجْزَرَةِ، وَالْمَقْبَرَةِ، وَقَارِعَةِ الطَّرِيقِ، وَالْحَمَّامِ، وَمَعَاطِنِ الْإِبِلِ، وَفَوْقَ ظَهْرِ بَيْتِ اللَّهِ. ۞

‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza **Kusali katika sehemu 7: Majaani, Machinjioni, Makaburini, Chooni, Njiani, Kwenye Mazizi ya Ngamia, Juu ya Paa La Msikitin**i*(Imam At Tirmidhii)*

Ambapo tunapozungumzia Kuhusiana na Njiani basi Wanasema Wanazuoni kua: ‘**Sababu ya Kukatazwa Kusali Njiani, ni Kutokana na Kua hua ni kwenye Kuwavunjia Haki zao Wapita Njia, na pia Humpelekea Mtu anaesali Kukosa Utulivu na Unyenyekevu.**’*(Mawsuat Al Fiqhiya)*

Juu ya Hili basi Wanazuoni wanasema pia Hairuhusiki kwa Mtu Kusali Njiani pale inapokua hakuna Udhuru kwa sababu kufanya hivyo hua Kunazuia watu kupita. Lakini kwa Mfano inapotokea Dharura kwa Mfano Kama katika Sala za Jamaa katika Msikiti ambao Watu ni wengi Sana, kiasi ya kua Wanajaa na Kusali hadi Nje mpaka Barabarani, basi hii hua Inakubalika na haina Madhara kaa sababu hua ni Dharura.

Hivyo Kusali katika Sehemu ambazo wanapita Watu au Njiani bila ya Dharura hua ni Makruh kulingana na Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Malik na Imam Al Shafii.

Kwani kwa maana hio basi Kama ikiwa ni Makruh kusali Njiani basi hua ni Makruh pia Kusali Mlangoni. Yaani kwa Mfano Kusali Sala ya Sunnah kwenye Mlango wa Kuingilia na Kutokea Msikitini na hii ni kwa sababu unakua unawavunjia Haki zao Watu wanaotaka kuingia na kutoka Msikitini. Na wengi wetu hua wanafanya hivyo aidha kwa kutojua au kwa kudharau.

SUJUD KATIKA SEHEMU YA ARDHI ILIYOPORWA

❖❖❖

Tunapozungumzia kuhusiana na Kupora Kitu basi hua tunazungumzia maana ya neno Ghasaba ambalo humaanisha Kuchukua Kitu kwa Nguvu, Bila ya Ridhaa, Kunyanganya kwa kutumia Nguvu, Kuchukua kitu kutoka kwa Mtu kwa Kulazimisha na Kuchukua kitu kwa Njia zisizokua za Haki.

Kama anavyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Surat Al Kahf pale Al Khidr alipomuelezea Nabii Musa sababu za Kulitoboa kwake Jahazi walilokua wakisafiria baada ya kupewa Msaada na wenye Jahazi kua:

﴿أَمَّا ٱلسَّفِينَةُ فَكَانَتْ لِمَسَاكِينَ يَعْمَلُونَ فِى ٱلْبَحْرِ فَأَرَدتُّ أَنْ أَعِيبَهَا وَكَانَ وَرَآءَهُم مَّلِكٌ يَأْخُذُ كُلَّ سَفِينَةٍ غَصْباً﴾

Amma alssafeenatu fakanat limasakeena yaAAmaloona fee albahri faaradtu an aAAeebaha wakana waraahum malikun ya/khudhu kulla safeenatin ghasban *(Sura tAl Kahf 18:79)*

Tafsir: ***(Akasema Al Khidhr kumwambia Nabii Musa)'Ama Kuhusiana na Jahazi, basi lilikua ni la Masikini waliokua wakifanyia kazi baharini, hivyo nilitaka kulitia kasoro, kwa sababu kabla yao kulikua kuna Mfalme ambae alikua akiliteka (akilipora) kila Jahazi kwa nguvu'***

Na ili utokee uporaji basi kwanza lazima kuwepo kwa Umiliki wa Kitu, na tunapozungumzia kuhusiana na Umiliki wa Kitu basi Kiislamu kua kuna aina mbili za Umiliki wa Kitu, kwani kuna Umuliki wa Kijamii juu ya kitu ambao uhusiano wake hua ni Jamii kwa ujumla na Kitu kinachomilikiwa na Jamii husika.

Na kuna Umiliki Binafsi wa Mtu juu ya Kitu ambao hua ni Uhusiano baina ya Mtu na Mali yake unaomuwezesha kukitumia kitu hicho au kukifanya anavyotaka bila ya kuingiliwa kati katika Utumiaji wa Mali yake kwa kuzuiwa kulingana na Sharia, na hivyo kuwazuia watu wengine kukitumia Kitu hicho au kukichukua kitu husika isipokua pale itakapotokea sababu ambayo hua ni kizingiti ambacho kinachokubalika kisharia na kumpelekea Mmiliki husika kuingiliwa kati katika hali ya utumiaji wa anachokimili.

Kwa mfano pale mmiliki atakapokua na matatizo ya kutokwa na Akili, Matatizo ya kusahau, matatizo ya kua ni Mtoto mdogo ambae bado hajatimiza Umri stahiki wa kuweza kusimamia anachokimiliki, kufanya Israfu kwa kutokana na Ujinga, n.k ambapo kutokana na sababu hizo basi Usimamizi wa Kitu chake hicho hua ni wenye kukabidhiwa kwa Mtumwenye Uwezo wa kusimamia kitu chake hicho kwa haki na kwa kisharia, kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَأْكُلُوٓاْ أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِٱلْبَاطِلِ إِلاَّ أَن تَكُونَ تِجَارَةً عَن تَرَاضٍ مِّنْكُمْ وَلاَ تَقْتُلُوٓاْ أَنْفُسَكُمْ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيماً﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo la ta/kuloo amwalakum baynakum bialbatili illa an takoona tijaratan AAan taradin minkum wala taqtuloo anfusakum inna Allaha kana bikum raheeman*(Surat An Nisaa 4:29)*

*Tafsir:****Enyi Mlioamini Msile Mali zenu baina yenu kwa njia zisizokua za haki isipokua pale itakapokua mmefanya biashara ya kubadilishana(kwa Pesa au kwa Mali) kwa makubaliano baina yenu, na wala msiuane Nafsi zenu, kwani kwa hakika Allah ni mwenye huruma Juu yenu.***

Na Uislam umeruhusu mtu kupigania haki yake, kiasi ya kua hata kama akifariki basi Mtu huyo hua ni sawa na aliefariki katika vita vya Jihadi kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Yeyote atakaefariki katika hali ya kua ni mwenye kupigania kuilinda haki yake basi hua ni shahidi'***(Sahih Al Bukhari)*

Ambapo haki ya Umiliki wa Kitu katika Sharia za Kiislam hua ni zenye kusimamiwa kwa kila Mtu bila ya kubagua kama Mtu husika ni Muislam ama la, ni Mgeni au ni Mwenyeji wa sehemu husika kulingana na Haki na Uadilifu wa Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama ilivyoamrishwa katika Qur'an pale iliposema:

﴿يَا أَيُّهَآ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ كُونُواْ قَوَّامِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلْقِسْطِ وَلاَ يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَآنُ قَوْمٍ عَلَىٰٓ أَلاَّ تَعْدِلُواْ ٱعْدِلُواْ هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo koonoo qawwameena lillahi shuhadaa bialqisti wala yajrimannakum shanaanu qawmin AAala alla taAAdiloo iAAdiloo huwa aqrabu lilttaqwa waittaqoo Allaha inna Allaha khabeerun bima taAAmaloona*(Surat Al Maidah 5:8)*

Tafisr: ***Enyi wale ambao Mlioamini kuweni ni wenye msimamo kwa ajili ya Allah na kuweni Waadilifu na wala msiuachie Uadui na Chuki baina yenu kukupelekeeni kua ni wenye kuiepuka haki. Kuweni Waadilifu kwani kua hivyo hua ni kuikaribia Taqwa na Muogopeni Allah, kwani kwa hakika Allah ni mwenye kua na habari juu ya kila mnachokifanya.***

Aya inazungumzia kuhusiana na Uadilifu, kwa sababu Uadilifu, hua ni wenye kileta Utulivu na Usalama katika Jamii, Kwani Uadilifu ndio Sifa kuu ya Kimaumbile ya Dini ya Kiislam. Ambapo anasema Al Faqih Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Muhamad Ibn Rushd Al Qurtubi Al Maliki Al Andalus kuhusiana na ayah hii kua: **'Hairuhusiki kulingana na ayah hii, kua pale itakapotokea Maadui wa Kiislam kua ni wenye Kuwatesa Waislam, au kuwaua Wanawake wa Kiislam na Watoto kuikata Miili ya Maiti wa Kiislam, basi na Waislam walipize kisasi kwa njia hio hio, kwani Uislam hauruhusu tabia za kinyama kama hizo.'**

Hivyo Uadilifu hua ni wenye kupatikana kutokanana kusimamia haki za Watu na Makubaliano baina yao katika Jamii, bila ya kujali Uadui baina ya Watu, wala tofauti za Kiimani wala uenyeji au ugeni,n.k.

Na tunapozungumzia Uporaji wa Kitu basi hua kuna aina Mbili Kisharia Kuna Uporwaji wa Kitu unaokubalika Kisharia na Kuna Uporaji Usiokubalika Kisharia. Na tunapoangalia Kulingana na Maqasid Al Sharriyah yaani Malengo ya Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi tunaona kua Uporwaji wa Kitu unaokubalika hua ni Ule wa Kupokonywa Mtu Kitu anachokimiliki kisharia kwa ajili ya Kusimamia Maslahi ya Jamii.

Ambapo anasema *Hujjat Ul Islami Imam* Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii Al Tusi kua: '**Kusimamia Maslahi ya Jamii hua ni Kusimamia Kile Kitakacholeta Manufaa kwa Jamii na Kuepusha Kile Kitakachosababisha Madhara katia Jamii.'**

Hivyo kwa upande wa Uadilifu kisharia basi **Uislam umeruhusu pia kwa mmiliki kupokonywa anachokimiliki na wenye Mamlaka kama ikiwa kupokonywa kwake huko kitu hicho kutaleta manufaa katika Jamii au kutaepusha madhara katika Jamii, pale itakapokua mwenye kumiliki kitu hicho amekataa kukiuza, ambapo baada ya kupokonywa kwake huo basi mmiliki huyo hua ni mwenye kulipwa fidia Stahiki badala yake**.*(Naz Al Mulkiyyah li Al Maslah Al Aa'ma)*

Ambapo hii hua inategemea na umiliki wa kitu husika, kwani kuna baadhi ya vitu katika Uislam hua hairuhusiwi kwa Mtu Binafsi kumiliki, ambavyo huanivile vitu vinavyotumika Kijamii kwa ujumla, kwa mfano, Bahari, Mito, Ziwa, Barabara, n.k na pia imekatazwa kumiliki vitu vilivyo haramishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kama Nguruwe, Vilevi, Kamari, Madanguro n.k.

Kwa maana hio basi hua inakubalika kwa wenye Mamlaka kuchukua sehemu ya kitu au kitu cha Mtu binafsi kwa nguvu kwa ajili ya Manufaa ya Jamii kwa ujumla, na kisha kumlipa Fidia stahiki mtu huyo, kama kitu hicho kitakua ni chenye kuruhusika kumililikiwa Kiislam, na kama hakiruhusiki basi hua hakuna fidya inayostahiki kulipwa, kutokana na kua kitu hicho ni haramu. hivyo inaruhusika Kuvunja Nyumba, au kuchukua eneo la Ardhi ya Mtu husika kwa ajili ya Kujenga Barabara, au kuitanua, kujenga Msikiti au Kuutanua, Kujenga Hospitali au Skuli n.k.

Hivyo tuangalie kulingana na Mitizamo mifano iliyochukuliwa kua ni kigezo cha kukubalika kwa uchukuliwaji wa nguvu wa kitu husika kutoka kwa mtu kwa manufaa ya jamii, ili japo kidogo tupate kufahamiana kuhusiana na Aina ya Ardhi husika kwani kuna Masuali yanaweza kujitokeza kwa Wengi Miongoni mwetu katika Jamii kutokana na Kutokua na Uhakika na sehemu wanazoishi na kujenga Miskiti pia kua zilipatikanwa vipi hapo kabla, yaani isije ikawa Mtu anasali kwenye Msikiti ambao Anasali miaka yote ndani yake lakini kumbe Asili ya Ardhi yake ni kua Iliporwa na watu hawakulipwa fidia baada yake.

Au Mtu anaishi ndani ya Nyumba miaka yote lakini kumbe Nyumba hio Wamiliki wake Waliporwa bila kulipwa fidia hapo kabla.Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya An Nawawi kua: '**Kusali Ndani ya Ardhi Iliyoporwa Kumeharamishwa na hii ni Kulingana na Makubaliano ya Wanazuon**i.'*(Al Majmuu)*

Miongoni mwa mifano Kuhusiana na Kuchukuliwa Kitu kwa Nguvu kwa ajili ya Maslahi ya Jamii na kisha wamiliki wao kulipwa fidia stahiki basi Wanazuoni wanachukua Mfano wa***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alipowasili Katika Mji wa Madina basi Ngamia wake alisimama kwenye alisimama kwenye eneo la Ardhi ya Mayatima wawili ambao niSahl na Suhail ambao walikua chini ya Uangalizi wa Asad Ibn Zurara *Radhi Allahu Anhu.***

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: '**Sehemu Hii Inshaa Allah ndio nitakayojenga Makazi yangu.'**

Hivyo Mayatima wawili hao wakaitwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaambia kua Wamuuzie sehemu hio ili ajenge Makazi yake na Msikiti.Na Watoto hao wakasema: 'La, Kukuuzia hatukuuzii ila tutakupa kama zawadi ya Rasul Allah.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaichukua sehemu hio kama Zawadi kutoka kwa Mayatima wawili hao,na kisha pia akawalipa.Hivyo hapa kimetumika Kiasi cha kulinganishana lazimisho la *Rasul Allah Salallahu* ***Alayhi wa Salam*** kutaka Kuuziwa eneo la Ardhi kwa ajili ya Manufaa ya Jamii lakini matokeo yake akagaiwa.

Mfano Mwengine ni wa Bustani ya Banu Najjar na alipoiona baada ya Mda akawaita Watu wa Banu Najjar na kuwaambia: **'Enyi Banu Najjar tajeni bei kwa ajili ya hii Bustani yenu.'**

Ambapo nao wakasema:**'Wa Allahi sisi hatutokubali bei kutoka kwa yeyote isipokua kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'**

Na *Rasul Allah SalallahuAlayhi Wa Salam* akaichukua Bustani hio na Masahaba wakuaisafisha na Makaburi ya Mapagani yalikuwepo hapo yakafukuliwa na kuhamishwa na Ardhi ikatumiwa kwa ajili ya Waislam.*(Sahih Bukhari)*

Na pia Mfano wa Kisima cha Rumah ambacho ilikua hakuna kisima chenye Maji Matamu katika Mji wa Madina zaidi Yake na Mmiliki wake alikua akiyauza Maji hayo.**Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Rumah *Radhi Allahu Anhu* kua : 'Jee Utakiuza Kisima chako?'**

Rumah akasema: 'Wallahi Ya *Rasul Allah* nnaapa mimi kua mimi na Familia yangu tunakitegemea Kisima hiki kwa kila kitu.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaambia Masahaba zake: 'Jee ni Nani atakaekinunua Kisima hiki kwa ajili ya Kisima bora zaidi Peponi?**

Ambapo Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* akakinunua na Kukitoa Sadaka kwa Waislam.*(Imam At Tirmidhii)*

Hivyo basi kulingana na Mifano hii ya Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tunaona kua hua Inakubalika Kutumia Nguvu kuchukua Mali ya Mtu mmoja kwa ajili ya Manufaa ya Jamii kwa Ujumla.

Hivyo kama tulivyoona kulingana na Mifano ya Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua hua Inakubalika Kutumia Nguvu kuchukua Mali ya Mtu mmoja kwa ajili ya Manufaa ya Jamii kwa Ujumla au kwa ajili ya Kuondosha Madhara katika Jamii Husika kwa Ujumla. Lakini hua ni lazima kwa Mtu huyo alienyang'anywa Kitu chake alipwe Fidia badala yake.

Ambapo kama tulivyoona kua kwa upande wa Kipindi cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Masahaba walipoamrishwa Watoe Mali zao kwa ajili ya Manufaa ya Jamii kisha walipwe Fidia basi wengi wao wakikataa na kusema kua kwao ni Bora Kufanya Biashara na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuliko kulipwa Fidia.

Na Miongoni mwa Matukio kama hayo lilikuwepo pia lile lililotokea katika wakati wa Utanuzi wa Masjid An Nabawi Madina katika wakati wa Utawala wa *Amir Ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*Hivyo ili kuutanua Msikiti huo basi ikabidi Zifunjwe Nyumba za Jirani yake na wamiliki wa Nyumba hizo wakalipwa Fidia. Ambapo Miongoni mwa waliokataa kutoa na Kuvunjiwa Nyumba yake alikuwepo Al Abbas Ibn Abd Al Muttalib *Radhi Allahu Anhu.*

Jambo ambalo lilipekekea kutokea Mgogoro baina ya *Amir ul Muumin* Umar Ibn Al *Khattab Radhi Allahu Anhu* na Al Abbas *Radhi Allahu Anhu.*Na Hivyo Kesi hio ikafika kwa Qadhi wa Mji wa Madina ambae alikua ni Sahaba Mwanazuoni wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aitwae Ubay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu.*

Na kesi ilipofika Mbele yake basi Ubay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* akatoa Fatwa kulingana na Kile kilichotokea katika **Wakati wa Uhai wa Nabii Daud alipoamrishwa Kujenga Msikiti katika sehemu ambayo kulikua kuna Nyumba ya Yatima wa Kiyahudi aitwae Andar.**

Hivyo Nabii Daud akamfuata Mtoto huyo na kumwambia kua: 'Ya Andar nimekuja kwako kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala*Ameniamrisha mimi kua Nijenge Msikiti kwenye Ardhi yako.'

Andar akasema: 'Inaamana unaniambia kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekuamrisha wewe Kuchukua eneo langu bila ya Ridhaa yangu?'

Nabii Daud akasema: 'La!'

Andar akasema: 'Basi Mimi sitaki na sitoi Ardhi yangu.'

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamuamriaha Nabii Daud kumlipa Andar Qintar moja Dhahabu kua kama Fidya ya Eneo lake hilo.

Nabii Daud alipompa Andar Dhahabu hio, Andar akasema: 'Nimesema sitaki Ardhi Yangu kuitoa.'

Nabii Daud akaongeza idadi ya wingi wa Qintar wa Dhahabu, na Andar akaendelea kukata, Nabii Daud akaongeza tena na tena hadi kufikia mara 9 zaidi ndio Andar akakubali Kutoa Ardhi hio na kuchukua Dhahabu hio.

Hivyo Al Abbas *Radhi Allahu Anhu* aliposikia habari hii basi akasema: 'Kama ni hivyo basi Mimi sitaki Fidia yeyoye bali natoa Nyumba yangu kama Waqf kwa Waislam.'

Hivyo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akakubaliana na Jambo hilo na Nyumba ya Al Abbas *Radhi Allahu Anhu* ikavunjwa na Msikiti wa Madina ukaongezwa Ukubwa na Upana wake.'*(Shadharat Al Dhahab)*

Tukio jengine ni lile lililotokea tena katika Utanuzi wa Msikiti wa Makkah na Madina katika wakati wa Utawala wa Amir Ul Muuminin Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu.*

Kwani baada ya Miji kukua na idadi ya watu kuongezeka basi Miskiti miwili hio ikawa tayari imeshakua Midogo watu wanajaa sana na wengine hata nje wanakosa nafasi. Hivyo *Amir ul Muuminin* Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* akaamua kuitanua Miskiti miwili hio na kuwalipa Fidia wale wataovunjiwa Nyumba zao kwa ajili ya Utanuzi huo.

Lakini Watu wa Mji wa Makkah na Madina wenye Nyumba za Jirani na Misikiti hio walikasirika na Wakakataa kuvunjiwa na pia kukakataa kuchukua Fidia.

Amir Ul Muuminin Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* akasema:**'Umar alipokuwepo katika Uhai wake alifanya hivyo na nyinyi Mlikubaliana nae.'**

Na ikabidi watu hao walazimike kukubali matakwa ya Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* wakalipwa Fidia, na Nyumba zikavunjwa na kisha Misikiti Ikaongezwa Upana.

Hivyo anasema Al Allamah Al Faqih Imam Ali Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii kua: '**Hii Inaonesha kua Inakubalika kwa Wenye Mamlaka Kuchukua Kitu kwa Nguvu pale itakapokua inahitajika Kufanya hivyo kwa Ajili ya Maslahi ya Jamii kwa Ujumla.'**

Miongoni mwa mifano ya Matukio kama haya basi kuna lile tukio la Bilal Ibn Al Harith Ibn Asim Ibn Said Ibn Qurrah Ibn Khalada Ibn Thalaba Al Mazani *Radhi Allahu Anhu* ambae alipewa Eneo la Ardhi na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Maeneo ya Qaballiyah na Karibu ya Mji wa Madina.

Lakini hata hivyo Bilal Ibn Al Harith *Radhi Allahu Anhu* alishindwa Kulisimamia Eneo hilo kikamilifu kutokana na Ukubwa wake. Hivyo katika Wakati wa Utawala wa *Amir Al Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*, akamfuata Bilal Ibn Al Harith *Radhi Allahu Anhu* na akazungumza nae kuhusiana na Umiliki wa Eneo hilo na Masharti yake Kiislam, hivyo akamwambia kua: '**Angalia sehemu ya Ardhi Utakayoweza Kuitumia katika Ardhi hii na kisha nitakuachia Itumie na ile itakayobakia ambayo huwezi Kuisimami basi Itakubidi Utupe sisi ili Tuigawe kwa Baadhi ya**

Waislam wengine waliokua wanaweza kuifanyia Kazi.' Hio iliyobakia, Lakini Bila al akaataa kuitoa na hivyo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akaichukua kwa Nguvu sehemu hio ya Ardhi iliyobakia na kuigawa kwa Waislam wengine.

Kwani vile vile katika wakati wa Mamlaka ya Utawala wa Khalifa Walid Ibn Abd Al Malik ambapo katika Wakati huo Gavana wa Mji wa Madina alikua ni Umar Ibn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhu* Ulifanyika Utanuzi pia wa Masjid An Nabawi hivyo Khalifa Walid Ibn Abd Malik alimtumia pesa Umar Ibn Abd Al Aziz ili anunue Nyumba za Jirani zivunjwe kuuongeza Msikiti.

Na Khalifa Walid Ibn Abd Malik akamwambia Umar Ibn Abd Al Aziz kua: '**Yeyote yule atakaeamua Kukuuzia Nyumba basi Mlipe Kiasi fulani, na atakae kataa kuuza basi Nyumba yake Ivunje kisha Mlipe Fidia yake kama alieuza NyumbaNa Kama Mtu akikataa Kuuza na akikataa Kuchukua Fidiya ya Pesa hizo pia basi Chukua Pesa hizo kisha zitoe Sadaqah kwa Masikini.'***(Wafa Al Wafa Bi Al Akhbar)*

Na katika wakati wa Kipindi cha Khalifa Jafar Al Mansur basi Masjid Al Haram ilitakiwa kutanuliwa pia na ikabidi zinuliee Nyumba za Jirani kisha zivunjwe, na Baadhi ya Watu wakagoma Kuuza, na walikataa katu katu. Hivyo Khalifa Al Mansur akatafakkari kisha akamkumbuka Imam Jafar Al Sadiq.

Hivyo Khalifa Al Mansur akamfuata Imam Jafar Al Sadiq na kumuelezea Ugumu aliokutana nao katika Jitihada zake za kutaka Kuutanua Msikiti wa Makkah kwa Manufaa ya Ummah.Ambapo Imam Jafar Al Sadiq akamsomea Khalifa Al Mansur aya isemayo:

﴿إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِى بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَٰلَمِينَ﴾

Inna awwala baytin wu<u>d</u>iAAa lilnn<u>a</u>si lalla<u>dh</u>ee bibakkata mub<u>a</u>rakan wahudan lilAA<u>a</u>lameena*(Surat Al Imran 3:96)*

*Tafsir:**Hakika ya Nyumba ya kwanza Waliochanguliwa Watu(Kwa ajili ya Kuabudu)Ni Ile Ambayo Iliyokuwepo Katika Mji wa Bakkah (Makkah) Yenye Baraka na Uongofu kwa Ajili ya Walimwengu.***

Na kwa kua Masjid Al Haram ni Msikiti Mtukufu ambao ni bora kuliko Nyumba yeyote, kwani ndio Nyumba ya mwanzo Kuelekewa katika Ibada na unahitajika Kuongezwa basi Watu hao itabidi Wapishe Utanuzi huo wa Msikiti watake wasitake kwa Manufaa ya Ummah kwa Ujumla. Khalifa Al Mansur akataka kutokukubaliana na Ushauri wa Imam Jafa Al Sadiq na Hivyo Imam Jafar Al Sadiq akamwambia:**'Sawa, basi Fanya vyovyote vile Utakavyoamua kufanya.'**

Hivyo Wanazuoni wanakubaliana kua: '**Inaruhusika Kuchukua Kitu cha Mtu Binafsi kwa ajili ya Manufaa ya Jamii kwa Ujumla iwe kwa Ajili ya Kuuongeza Msikiti, Kutengeneza Barabara, Kutoa Huduma ya Maji, Umeme, Kujenga Skuli, Hospitali nk.Lakini pale inapokua Kuchukuliwa kwa Kitu hicho kutakua ni kwa Haki kulingana na Sharia na Kulipwa Fidia Stahiki badala yake.'**

Ambapo anasema Imam Kamal Ad Din Muhammad Ibn Abd Al Wahid Ibn Hammam Al Hanafi Al Maturidi kua: '**Kama Msikiti Utakua Mdogo na kuna Eneo Pembeni yake ambalo Lina Duka labda basi inakubalika Kuvunja Duka Kuongeza Msikiti, hata kama Mwenye Duka atakubali bila Kutaka kuchukua Kiasi cha Fidiya, na hata kama ikiwa ni kwa Ajili ya Barabara pia'***(Fat-h Al Qadir)*Na huo pia ndio Mtizamo wa)Sayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafi katika *Khashiyat Radd Al Mukhtar.*

Na si kuhusiana na Viwanja tu bali pia tunapozungumzia kuhusiana na vitu tofauti kwa mfano Vyakula, kwa Mfano kama Kuna '**Mfanyabiashara Ameficha Chakula na Ili akiuze kwa Bei Ghali baadae na Katika Mji hakuna Chakula basi Kiislam hua Inaruhusika kwa wenye Mamlaka Kumnyang'anya Alieficha Chakula husika na kisha Kukiuza kwa ajili ya Kuondoa Madhara ya Shida ya Chakula Husika katika Jamii**'*(Al Ashbah wa Al Nazair)*

Kwani kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik basi Wanazuoni wao wanakubaliana juu ya Mambo yafuatayo:

Inakubalika Kumlazimisha Mwenye Maji Kumuuzia mtu Mwenye Kiu, Mwenye Shamba ambalo Mazao yataharibika bila Maji hayo,n.k.

Inakubalika Kumlazimisha Mwenye Ardhi kuizua Ardhi kwa ajili ya Masikiti itakapohitajika.

Inakubalika Kumlazimisha Mtu mwenye kumiliki sehemu ya Juu ya Mji husika kwa ajili ya Kujenga Ngome ya Ulinzi wa Mji, nk.

Ambapo Mitizamo Yote hio pia Inakubaliwa na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Inafaa Kuyapa Kipaumbele Mahitajio Muhimu zaidi ya Jamii katika Jamii kisha ndio Mahitajio ya Mtu Binafsi *(Qawaid Al Ahkami Fi Masail Al Anam)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Abu Amr Uthman Ibn Abd Rahman Salah Ad Din Al Kurdi Al Sharhazuri Al Shafii basi yeye anasema kua:**'Inakubalika kwa Mtu yeyote ambae amenunua Mtumwa na Kisha akamlazimisha Kufanya Biashara ya Kuuza Mwili wake kua Amuachie Huru Mtumwa huyo, na pia Inaruhusika Kumlazimisha Mtu Mwenye Mfanyakazi ambae anamfanyisha Kazi Ngumu sana bila ya Huruma, hivyo inafaa Kumlazimisha Mwenye Mfanyakazi huyo Kumwachia huru Mfanyakazi husika kwa ajili ya Kumlinda Mfanyakazi kutokana na Unyanyaswaji**'*(Al Ashbah wa Al Nazair)*

Hivyo Maslahi ya Jamii yamepewa Kipaumbele zaidi kuliko ya Mtu BinafsiKwani inapodhurika Jamii basi hua ni Madhara makubwa zaidi kuliko anapodhurika Mtu Binafsi, na hivyo hua ni bora kutaifishwa Kitu cha Mtu Binafsi na Kulipa Fidia kwa ajili ya Manufaa ya Jamii kwa ujumla.

Na kwa Upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi yeye '**Alikubaliana na Mtizamo wa kama alivyofanya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* pale alipolazimisha Kuuziwa Ardhi kwa ajili ya Kujenga Jela, Kwani Kuwaweka Jela Wenye Hatia hua ni Kuwezesha Kupatikana Usalama, Utulivu na Amani katika Jamii.'**

Na kwa upande wa Imam Ibn Al Qayyim basi yeye alisema pia kua '**Inaruhusika kwa mwenye Kutengeza Silaha Kulazimishwa kuziuza pale zitakapohitajika kwa ajili ya Vita vya Jihad.'**

Kwani Moja kati ya Kanuni za Fiqh ni yenye Kusema kua:

***Al Maslaha Al Ammah Tuqaddam aAla Al Maslaha Al Khasah* - Maslahi ya Ummah yana kipaumbele zaidi Ya Maslahi ya Mtu Binafsi.**

Na nyengine inasema:
***Al Dharurah Tubihu Al Mahzurat* - Dharura Huruhusu kilichokatazwa.**

Na Nyengine inasema**:**
***Al Dharar Al Ashadd Yuzal Bi Al Dharar Al Akhaf* - Dhara Kubwa linakubalika kuondolewa kwa Kupitia Dhara Dogo.**

Na Kuna isemayo kua:
***Ma La Yatim Al Wajib Ila Bihi Fahuwa Wajib* - Jukumu lisipotimizwa bila Kuwajibishwa basi Inabidi Kuwajibishwa.**

Hivyokatika Ardhi zilizotaifishwa na wenyewe wakapewa fidia stahiki hua inakubalika kusujud ndani yake, na hua ni tofauti na ile Ardhi ambayo hairuhusiwi Kusujudu ndani yake au juu yake kutokana na kua hua ni sehemu Ardhi ambayo Imeporwa kwani wenyewe hawakulipwa chochote, na hivyo hua ni Haramu kuishi ndani yake basi imekua ni Haramu pia Kusujudu na Kusali ndani yake.*(Al Mawsoo'ah Al Fiqhiyyah)*

Kwani amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua**:**

أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ مَنْ اقْتَطَعَ شِبْرًا مِنْ الْأَرْضِ ظُلْمًا طَوَّقَهُ اللَّهُ إِيَّاهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مِنْ سَبْعِ أَرَضِينَ

Amesema*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Atakaechukua Sehemu ya Ardhi ya Ndugu yakekwa kudhulumu basi atabebeshwa Ardhi 7 za sehemu hio shingoni mwake katika siku ya Malipo'*(Imam Bukhari)*

Ambapo hii ni Hadith ambayo imeifanya Sehemu ya Ardhi iliyoporwa yaani iliyopatikana kwa njia ya Kudhulumiwa Mtu kua ni sehemu ambayo Haramu, kutokana na kua imepatikana kwa njia ya Dhulma na hivyo kua ni Haramu hata kuishi ndani yake.

Na hivyo wanasema Wanazuoni kua: '**Ni Haramu Kusali ndani ya Sehemu Iliyoporwa kwa sababu ya Kuharamishwa kwa Ardhi hio Nje ya Sala, kwa maana huo basi Hata Kuingia Ndani ya Sala katika Ardhi hio Kumeharamishwa kwa sababu Kubwa Zaidi' (*Al Mawsuah Fiqhiyyah)***

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُم بَيْنَكُم بِالْبَاطِلِ وَتُدْلُوا بِهَا إِلَى الْحُكَّامِ لِتَأْكُلُوا فَرِيقًا مِّنْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْإِثْمِ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ﴾

Wala ta/kuloo amwalakum baynakum bialbatili watudloo biha ila alhukkami lita/kuloo fareeqan min amwali alnnasi biAl ithmi waantum taAAlamoona.*(Surat Al Baqara 2:188)*

*Tafsir**: Na Wala Msiliane Mali zenu baina YenuKwa Njia zilizobatili na wala Msitumie Hongo Kwa Mahakimu Kwa Ajili ya Kula Kutoka katika Sehemu ya Mali ya Watu wengineKwa DhambiHuku Mkiwa Mnajua***

Ambapo Aya hii Inathibitisha kua Kumuliki Kitu cha Mtu Mwengine kwa njia za Batili hua ni Miongoni mwa Dhambi kubwa.Na katika Kusisitiza hili basi amesema tena *Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam*

kua: **Hatakiwi hata mmoja Miongoni mwenu Kua ni mwenye Kuchukua Mali ya Mwenzake kwa Utani au kwa Ukweli, Hivyo atakaechukua Mali ya Mwenzake basi anatakiwa Airudishe'***(Imam Abu Daud)*

Na anasema Al Imam Shams Ad Din Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini Al Shafii kua: '**Mbali ya Kutakiwa Kurudishiwa Ardhi yake Mtu iliyoporwa lakini pia Kila kilichomo ndani yake kinatakiwa Kurudishwa kama kilivyokua, na kama yalitokea Maharibiko basi yanatakiwa yalipwe fidia, na kama kumeongezwa kitu basi kitolewe na pia inatakiwa alieporwa alipwe pia faida iliyopatikana ndani ya Kipindi chote cha mda alioporwa.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Kwa maana hio basi Msikiti uliojengwa Kwenye sehemu ya Ardhi iliyoporwa, basi hua unaingia katika hali ya kupatikana kwa njia za Kupora, na hivyo hua haifai Kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* wala Kusali ndani yake, mtihani ni kua sehemu nyingi za Ardhi hususan katika maeneo ya Zanzibar kuna watu waliporwa Mashamba yao na kutaifishwa katika kipindi cha Mapinduzi na kisha Serikali ikazigawa kwa watu wengine, na pia kwa upande wa Tanzania Bara kuna Ardhi na Nyumba ambazo zilitaifishwa baada ya kupokonywa wamiliki wake na kugaiwa kwa Watu wengine katika wakati wa kipindi cha baada ya Uhuru.

Ambapo amesema Sultan Al Ulamaa, Shaykh Ul Islami Al Imam Abu Muhammad Izza Ad Din Abd Al Aziz Ibn Abd Salam Ibn Abi Qasim Ibn Hasan Al Sulami Al Shafii kua: **'Kama Mtu ataingia Msikitini hukuakiwa na Nia ya Kutaka Kukaa Itiqaf Msikitini na kisha baada ya kukaa kwake ndani ya Msikiti huo akagundua kua Msikiti husika Umejegwa ndani ya Ardhi iliyoporwa, basi Itiqafyake Hubatilika hapo hapo.** *(Qawaid Al Ahkam)*

Na hii ni kwa Sababu Wanazuoni wanakubaliana pia kua: '**Kusali Ndani ya Msikiti Uliojengwa kwenye Ardhi Iliyoporwa hua hakuhusiani na Ibada zifanyikazo ndani ndani yake Hivyo Mtu akifanya Ibada ndani yake Ibada yake Itakubalika na atalipwa kua amefanya Ibada Husika, Lakini ataandikiwa Dhambi pia kwa sababu ya kua ameifanyaIbada husika Katika sehemu hio iliyoporwa.'**

Ambapo huu ni Mtizamo wa Wengi Miongoni mwa Wanazuoni. Lakini kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wanasema kua: '**Ibada inayofanywa Katika Ardhi Iliyoporwa hua ni Batili, Hata iwe imefanywa na Watu wangapi, na hii ni kwa sababu Ibada hio imefanywa katika Njia zilizokatazwa, na hivyo hua Batili yaani kwa mfano kama vile ambavyo inavyokua Ibada ya Sala au Funga ya Mwanamke aliekua Katika siku zake** *(Mawsuah Al Fiqhiyyah)*

Ambapo anasema Imam Al Hakim Al Tirmidhi kua**: 'Mimi nimejizuia kunywa hata maji kutoka kwenye Mto kwa kujiambia kua: 'Huenda Maji haya yakawa yametirikia katika sehemu ambayo ni ya Haram, hivyo nikawa ni mwenye kunywa Maji kutoka kwenye Visima tu na Mahodhi Makubwa makubwa tu.''**

KUSALI NA KUSUJUDU JUU YA KITU KILICHOTANDIKWA

❖❖❖

Baada ya kuangalia kuhusiana na Mifano ya vithibitisho vinavyoonesha kua haikubaliki Kujusudu juu ya Ardhi Iliyoporwa kutokana na hali ya Uharamu wake katika kuporwa kwake bila ya kulipwa fidia walioporwa na pia mifano inayoonesha kukubalika Kusjudu katika Ardhi iliyoporwa na kisha ikalipiwa

Fidia baada yake.Hivyo tunaendelea kwa tunaangalia kukuhusiana na Kusjudu Juu ya Kitu kilichotandikwa.

Kwani hapo awali tulizungumzia kuhusiana na Kutokubalika Kusjudu Juu ya Nguo au Kitu ambacho amekivaa Mtu katika Sala yake lakini hakijashikamana na Mwili wake, na tukaona kua pia kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wengine basi ni kua hua inakirihisha kufanya hivyo.

Lakini tunapoangalia kuhusiana na Kusujudu juu ya Kitu kilichotandikwa chini na hivyo hua kimetulia na hakifuatani na mienendo ya Hatua za Mwenye Kusali basi tunaona kua anasema *Ummu ul Muuminina* Maymuna Bint Harith *Radhi Allahu Anha* kua:'**Wakati nilipokua kwenye Siku zangu, Mimi nilikua si Mwenye Kusali,lakini nilikua nikikaa kwenye Jamvi pembeni ya Masjid Nabawi.Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Kwenye Khumra yake na katika Kusjudu kwake basi baadhi ya Nguo zake zilikua zikinigusa mimi.'***(Imam Al Bukhari)***

Ambapo *Khumra* hua ni sehemu ya Msala wa Kijamvi kilichosukwa kwa Majani ya Mtende ambacho hua Kinawekwa katika Sehemu ya Paji la Uso na hufikia hadi katika sehemu ya kuwekea Mikono katika Sijda.

Hivyo baadhi ya Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Bila ya kutandika Kitu chochote na Masahaba zake na baadhi ya wakati alikua akitumia *Khumra* kwa ajili ya Kujihifadhi Dhidi ya Baridi au Joto la Ardhi kulingana na hali ya mazingira ya mabadiliko ya hali ya Hewa na pia kulingana na sehemu anayosali.

Ambapo kwa Upande wa Imam Abu Sulayman Hamd Ibn Muhammad Ibn Ibrahim Al Khattabi Al Busti Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Khumra Inaweza Ikawa Kubwa zaidi ya sehemu ya Kuwekea Kichwa na Mikono katika Hivyo baadhi ya Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Bila ya kutandika Kitu chochote na Masahaba zake na baadhi ya wakati alikua akitumia Khumra kwa ajili ya Kujihifadhi Dhidi ya Baridi au Joto la Ardhi kulingana na hali ya Hewa.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Abu Sulayman Hamd Ibn Muhammad Ibn Ibrahim Al Khattabi Al Busti Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Khumra Inaweza Ikawa Kubwa zaidi ya sehemu ya Kuwekea Kichwa na Mikono katika wakati wa kusujudu na hii ni kutokana na Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema:**

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللهِ بْنُ مُحَمَّدٍ، قَالَ: حَدَّثَنَا عَمْرُو بْنُ طَلْحَةَ، قَالَ: حَدَّثَنَا أَسْبَاطٌ، عَنْ سِمَاكِ بْنِ حَرْبٍ، عَنْ عِكْرِمَةَ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ: جَاءَتْ فَأْرَةٌ فَأَخَذَتْ تَجُرُّ الْفَتِيلَةَ، فَذَهَبَتِ الْجَارِيَةُ تَزْجُرُهَا، فَقَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم: دَعِيهَا، فَجَاءَتْ بِهَا فَأَلْقَتْهَا عَلَى الْخُمْرَةِ الَّتِي كَانَ قَاعِدًا عَلَيْهَا، فَاحْتَرَقَ مِنْهَا مِثْلُ مَوْضِعِ دِرْهَمٍ، فَقَالَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم: إِذَا نِمْتُمْ فَأَطْفِئُوا سُرُجَكُمْ، فَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَدُلُّ مِثْلَ هَذِهِ عَلَى مِثْلِ هَذَا فَتَحْرِقُكُمْ.

AmesemaAbd Allahi Ibn Muhammad, kua amesema Umar Ibn Talha, kua amesema Asbat kua amesema Simaki Ibn Harbi kua amesema Ikrimah kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua amekaa juu ya Khumra na mara

akatokea Panya, ambae alianza kuuvuta Utambi wa Taa, na Mjakazi wa *Rasul Allah SalallahuuAlayhi wa Salam* akakaribia na kutaka kumzuia Panya huyo.

Lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamkataza kwa kumwambia: 'Muachie' Hivyo Panya huyo akauangusha Utambi huo kwenye Khamra na ikatoboka kwa kiasi ya ukubwa wa duara la Dirham moja. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Mkienda Kulala Zimeni Vibatari kwani Shaytani huviongoza Vitu kama hivi na kisha Vitakuunguzeni*(Imam Abu Daud)*****. Hivyo basi Khumra huweza kua Kijamvi chenye Ukubwa kama wa Msala pia.'**

Ama kwaupande mwengine basi tuaona kua Safari Moja Khalifa Abd Rahman Al Mahdi alienda katika Ardhi ya Madina, hivyo kwa kua yeye alikua ni Khalifa wa Utawala wa Al Abbasiyah wa Baghdad na kutokana na Wadhifa wake basi Watu wa Madina wakamtandikia Zulia Msikitini ili atakapoingia basi Asali juu ya Zulia.

Lakini Imam Malik ambae ndie aliekua Imam wa Msikiti wa Madina na Qadhi na Mufti wa Mji huo basi akakataza Kutandikwa kwa Zulia hilo na akaambiwa kua:**'Huyu anaekuja ni Khalifa hivyo inabidi Atandikiwe.'**Ambapo Imam Malik akasema:**'Liondoeni Hivi Jee Hamjui Nyinyi kua Kutandika Zulia Msikitini kwetu ni Bidaa?'**

NaImam Malik alisema hivyo kwa sababu katika Kipindi cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* basi Ilikua hakujatandikwa Mabusati ndani ya Msikiti wa Madina wala wa Makkah wala Miskiti ya maeneo Mengineyo, hivyo Misikitini walikua wakisali chini kama tulivyoona katika Hadith kadhaa hapo kabla.

Kwa Maana hio basi Kusali kwenye Mazulia kama tufanyavyo sisi leo hua ni Bidaa ya kweli, na Imam Malik yuko Sahih.

Lakini hata hivyo Hii ni Bidaa Hasana yaani ni Bidaa nzuri na hivyo hua ni Bidaa inayoruhusiwa, kwa sababu hakuna Ubaya ndani yake kusali na kusjudu juu ya Mazulia au Misala bali kuna uzuri wa kua ni Jambo lenye kumuwezesha Mtu anaesali Kusujudukwenye sehemu safi na kwa Utulivu zaidi, na pia kua na Uhakika wa kua Nguo zake hazitochafuka kwa vumbi n.k mbali ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* hawakufanya hivyo.

Kama tulivyoona katika Hadith ya *Ummu Ul Muuminina* Maimuna Bint Harith *Radhi Allahu Anha* kuzungumzia Khumra - Msala ambao *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiutumia Nyumbani.

Na kama ilivyofafanuliwa hadith hio katika Awn Al Ma'bud Sharh Sunna Abi Daud kua: '**Hadithi hii inaonesha kua Neno Khumra Linaweza kikatumiwa pia kumaanisha Msala mkubwa, kama ilivyosemwa kwenye Al Nihayat.'**

Ambapo kwa Imam Muhammad Ibn Ali Ibn Abd Allah Al Shawkani basi yeye amesema kua: '**Hadith hii inaonesha kua hakuna tatizo kusali juu ya Mkeka wa Kusalia iwe umeshonwa kwa Kitambaa, Makuti au kitu chengine chochote kile, iwe Mkubwa au Mdogo, iwe kama Msala au Kama Busati kwa Sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali juu Misala, Juu ya Ngozi za Wanyama n.k.'**

Kwani amesema Abu Said Al Khudry *Radhi Allahu Anhu* kua:

عن أبي سعيد الخدري : أنَّه دَخَلَ على النبيِّ صَلّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ قالَ: فَرَأَيْتُهُ يُصَلِّي على حَصِيرٍ يَسْجُدُ عليه

‘Nilimuona Mimi*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisali Juu ya Mkeka uliosukwa kwa Majani ambao alisujudu juu yake. Na nilimuoma Akisali hukua akiwa amevaa Nguo Moja tu ambao pembe zake zimepishana kwenye Mwili wake.’*(Sahih Muslim)***

Na amesema *Umm ul Muuminina Aisha Radhi Allahu Anha* kua:

كُنْتُ أَنَامُ بَيْنَ يَدَيْ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ، وَرِجْلاَيَ فِي قِبْلَتِهِ ، فَإِذَا سَجَدَ غَمَزَنِي ، فَقَبَضْتُ رِجْلَيَّ ، فَإِذَا قَامَ بَسَطْتُهُمَا

‘Mimi nilikua nimelala mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.Huku miguu yangu ikiwa baina yake na baina ya Kibla pale alipokua akisujudu alikua akinibana nami nikaikunja Miguu yangu, na alipokua akisimama basi huinyoosha: Katika wakati huo ilikia hakuna Taa ndani ya Nyumba yetu*(Sahi Bukhari)*

Ambapo Imam Abd Rahman Ibn Aad Ibn Rajab Al Hanbali katika kuifafanua Hadith hii basi amesema kua:

هذا يدل على أنه كان يسجد على طرف الفراش الذي كانت نائمة عليه ، وكانت رجلاها عليه

Hadith hii Inaonesha kua *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* alikua akisujudu Mwishoni Mwa Tandiko la Kitanda ambalo Aisha Radhi *Allahu Anha* alikua amelala juu yake, na hivyo Miguu yake yote ilikua pia juu ya Tandiko. *(Fat-h Al Barr Sharh Sahih Al Bukhari)*

Hivyo mbali ya kua Katika Wakati wa Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hadi katika wakati wa Masahaba, Tabiina na Tabii Tabiina ilikua hakutandikwi kitu Misikitini kama tulivyoona kwenye kauli ya Imam Malik.Lakini hata hivyo Kusujudu Juu ya kitu kilichotandikwa kama vile Zulia, Busati, Jamvi n.k Msikitini, Nyumbani, au katika sehemu yeyote ya kusalia kama vile hua inafaa kulingana na vithibitisho tulivyoviangalia.

Ila kwa sharti la kua Paji la Uso ni lazima Lididimizwe katika sehemu ya Kusujudia. Hivyo Paji hili la uso linatakiwa Liuhisi Uzito wa Mwili utokao kwenye Mabega katika Kusujudu.Na hii ni kwa sababu, kama Mtu atakua anasujudu kwenye Zulia lililoshiba Manyoya na kisha kichwa chake akawa hajakikandamiza kwenye Zulia hilo basi Paji la Uso litakua Linaelea Juu ya Zulia, ambapo Jambo hili litaifanya Sijida ya Mtu husika kua Batili.

Kama alivyosema *Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din* Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: ‘**Haitoshelezi kwa Paji la Uso kua ni lenye Kugusa kwa juu juu tu ya Ardhi ambayo mtu anaesali hua anasujudia, bali inatakiwa Kichwa chake kithibitishe kwa kuwepo kwa Uzito wake na Shingo ihisi kua Kichwa Kimekaa na Kimetulia hasa juu ya Sehemu ya Kusujudia Na wala isiwe kinagusa Tu sehemu hio**. **Hivyo kama mtu anasjudu juu ya Sehemu iliyotandikwa, labda kwa Pamba (Zulia) au Majani Makavu (Jamvi, Mkeka) basi anatakiwa aweke Kichwa chake kiasi ya kua uzito wake utadidimiza Pamba hio na kuacha athari ambayo kama Kwa mfano ingekua**

kumewekwa Mkono chini ya Pamba hio basi mkono huo uhisi athari hio ya Sujudu, na kama haikua hivyo basi hua haitoshelezi Sujudu yake hio.'(*Al Majmuu)*

Na kama alivyosema Imam Hasan Al Kaff Al Shafii kua: '**Ni Sharti la lazima kua Mti anaesujudu anatakiwa kukandamiza Paji lake la Uso kwenye sehemu anayosujudu kiasi ya kua kama atakua anasujudu juu ya Sufi basi atakaponyanyuka iwe Sufi hio imemganda kwenye Paji la Uso.'***(Al Takrirat Al Sadida fi Masail Mufida)*

Hivyo mbali ya kua inakubalika Kusjudu juu ya Matandiko yanayotandikwa kama Mazulia, Misala, Mikeka, Majamvi, Makapeti, Makaratasi, n.k, Lakini hata hivyo si Matandiko yote hua ni yenye kukubalika Kusujudia Juu yake, kama wanavyosema Wanazuoni kua: '**Inakubalika Kusali na Kusujudu Juu ya Matandiko yenye Picha kama zenye Vitu visivyokua na Uhai kama Bahari, Mito, Maziwa, Miti, Maua, Majengo n.k, Lakini hua ni Makruh, kwa sababu Huondoa Khushuu.'**

Lakini Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema)Sayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafikua: '**Inaruhusika Kusali kwenye Msala ambao una picha za Viumbe hai lakini pale inapokua picha zipo katika sehemu za kuwekea Miguu, na si sehemu ya Kusujudia kwa sababu hii hua ni sawa na Kufanya Unyanyasaji wa Picha kama hizo'***(Al Hidaya Al Aaliya)*

Na Muhimu ni kua tandikio hilo liwe safi katika sehemu ya Kusalia, Na anasema Shaykh Ul Islami Abu Zakkariyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi kua: '**Kama ikiwa kuna Najis katika Katika Zulia, Au Msala n.k, na kisha Mtu anaesali anasali kwenye sehemu yenye Najis hio basi Mtu huyo Sala yake hua ni Batili**, **Ila kama atakuwa anasali Katika Msala au Zulia hilo hilo lakini katika Upande ambao ni Safi na hauna Najis basi Sala yake Mtu huyo hua Sahih.'**

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Wanasema As-habi wetu kua hii hua bila ya Kujali kama Msala huo Unafuatana nae au haufuatani nae Mtu huyo anaesali katika Vitendo vyake vya Sala, na hii ni kwa sababu Huyu Mtu katika Kusali kwake hua si mwenye Kugusana na Najis hio**. **Hili pia Huhesabiwa kwa Mtu ambae anasali Juu ya Kitanda Ambacho Miguu ya Kitanda Imegusa Najis basi Sala yake hua Sahih, hata kama Godoro litakua linapanda na kushuka katika Hatua zake.'***(Al Majmuu)*

Na pia kuna Misala ambayo Kila Unaposujudu hua inakuhesabia Umesujudu Sijda ngapi ili usisahau, aina hii ya Misala pia hua haifai, kwa sababu Inamtoa kabisa Mtu kwenye Khushuu.Kwa maana hio basi Misala, Mazulia, Maboksi (Kwa wale wanaochelewa na kutowahi nafasi Misikitini na kisha akachukua Pande la Boksi akajiwekea Mbele yake na kusalia), n.k yasiyoruhusika Kusalia na Kusujudia hua ni yenye Aina za picha mbali mbali ikiwemo za Viumbe hai, kwa sababu zinapokua katika sehemu za Kusjudia basi hua ni sawa na Kuvisujudia viumbe hai hivyo.**Na Hivyo Hukmu yake hua ni Makruh (Vinakirihisha).**

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'aala* katika Quran baada ya *Bismi Allahi Rahmani Rahiim:*

﴿بِسْمِ اللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۞ يَٰٓأَيُّهَا ٱلْمُدَّثِّرُ ۞ قُمْ فَأَنذِرْ ۞ وَرَبَّكَ فَكَبِّرْ ۞ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ﴾

Ya Ayyuha Al Muddaththiru; Qum Fa-Andhir; Wa Rabbuka Fakabbir; Wa Thiyabaka Fattahir*(Surat Al Muddaththir 74:1-4)*

*Tafsir:**Ewe Uliejifunika Gubigubi. Nyanyuka Uonye. Na Mola Wako Umkuze kwa KumtukuzaNa Nguo zako Zitoharishe.***

Tuko katika kumalizia kuhusiana na Sujud na sehemu zinazoruhusika na zisizoruhusika kusjudia.Na ingawa nimeanza na aya ya 1 ya Sura hii lakini Malengo ni kuifafanua aya ya 4 ya Sura hii, na kam ilivyo kawaida ni kua ili watu wakifahamu vizuri zaidi unapoizungumzia Aya husika basi kwanza inabidi uangalie Mada ya aya husika imeanzia wapi.

Ambapo kwa upande wetu basi tunaona kua aya hizi 4 ni zenye kumwambia *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* kua Yanayomtokea katika Wakati huo ndani ya Maisha yake yalikua ni Maandalizi ya Kubebeshwa Jukumu kubwa kuliko yote aliyowahi kupewa Kiumbe Ibn Adam la kusimamia Kuufikisha Ujumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Walimwengu wote.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam* anaambiwa kua sio kama alikua anaota bali umfikiao ni ukweli halisi Na anatakiwa aamke, atokwe na khofu na kisha aanze Kuwausia Watu kuhusiana na Ujumbe huo wa Haki, na Kumtukuza*Allah Subhanah wa Ta'ala* kiukamilifu na katika Kumtukuza kwake huko basi anatakiwa awe katika hali ya Usafi.

Na Anasema Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkamilim, Imam Al Mushaqqiqin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na aya hii ya 4 kua: '**Matumizi ya Neno Fattahir katika aya hii yanajumuisha Utoharishaji wa Nguo na wa Kinafsi, na hivyo pia kumaanisha amrisho lisemalo: Usafishe Moyo wako kutokana na kila Ovu.'**

Ama kwa upande wa Jarrah Allah, Sultan Al Balagha Imam Abu Qasim Al Zamakhshari Basi yeye anasema kua: **Maneno Wathhiyabaka Fattahir yanatokana na usemi maarufu wa 'Tahir Athiyab' yaani Mtu ambae ni Msafi wa Kimavazi Kuelezea Sifa Nzuri**. **Kama vile inavyokua kwa Mtu ambae ni Mchafu kimavazi kuitwa 'Danis Ath Thiyab' na hivyo Kutilia Mkazo tofauti baina ya 'Usafi wa Kutokana na Kuasi na Kufanya Maovu na Uchafu wa Kukosa Ustaarabu na Kutokua na Imani'**

Na baada ya kuangalia Maana ya Aya kulingana na Mitizamo ha Wanazuoni Wakuu wa Ilm ya Tafsir ya Qur'an basi tunarudi katika Upande wa Fiqh ili kuangalia kuhusiana na maana ya Aya hii inasemaje?Ambapo nako tunaona kua Wanazuoni wameichukulia aya hii kua ni kithibitisho cha kua: '**Ili Sijida na Sala ya Mtu ikubalike basi Lazima katika Sehemu anayosujudia na Kusalia iwe Safi na Tohara, na hivyo Kama Mtu Atasujudu Au Atasali katika Sehemu Ambayo Si Tohara, Juu ya Kitu ambacho si Tohara, Akiwa na Kitu ambacho si Tohara, Akiwa na Mwili Si Tohara basi Sijda yake na Sala yake hio itakua Batili.'**

Kwani anasema Shayh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibm Sharaf An Nawawi kua: '**Mtizamo wetu ni kua Kutokua na Uchafu hua ni Sharti la Sala kua ni yenye Kukubalika, Iwe Sala Ya Sunna au Fardhi , Iwe ya Jeneza Au Sijida ya Kisomo cha Qur'an, Au Sijida ya Shukurani kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* .Hivyo Kutokua na Uchafu Kunahitajika katika Kila moja kati ya Hali hizi. Huo ndio Mtizamo wetu, mtizamo wa Abu Hanifa, wa Ahmad IbnHanbal na wa Wanazuoni wote waliotangulia Na wengineo.'**

'Na ingawa kuna Riwaya Tatu kutoka kwa Madhhab ya Imam Malik, ambapo Mtizamo unaokubaliwa zaidi ni kua Mtu anaesali (Anaesujudu) kama ikiwa atakua anajua kua Kuna Uchafu katika hali yake basi Sala (Sujud) yake hua ni Batili. **Lakini kama hajui au amesahau juu ya hilo basi Sala yake iko Sahih, na huo pia ndio Mtizamo wa Zamani wa Imam Al Shafii**. **Lakini**

Mtizamo wa *(Al Qawl Al Jaddid)* Kauli pya wa Imam Al Shafii ni kua Sala (Sujud) ya Mtu hubatilika iwe Mtu huyo hakujua juu ya uchafu huo au amesahau.' *(Al Majmuu)*

Ama kwa upande wa Imam Abu Ikhlas Ali Al Shurunbulali Al Hanafi basi yeye anasema kua: **'Kuhusiana na sehemu ya Kusalia basi sharti lake ni kua ni lazima iwe ni sehemu Tohara, hivyo Mtu anaweza kusali juu ya Ardhi tupu bila ya kutandika, au anaweza kusali juu ya kitu alichotandika lakin kiwe ni kisafi'**(*Al Maraqi a'l-Falah)*

Na kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Abd Rahman Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye anasema kua: **'Kama ikiwa Mtu atasali kwenye kitu alichokitandika ambacho kwenye cha yake kitakua kina Najis, au ikiwa chini yake kuna Kamba ambayo imefungwa kwenye kitu chenye Najisi, lakini kile anachokisalia ni Tohara basi Sala yake ni Sahih iwe kitu hicho alichokitandika kinatikisika pamoja nae pamoja na uchafu huo katika kila hatua za Sala yake ama la, na hii ni kwa sababu Uchafu huo haukuambatana nao kwenye nguo zake wala haukuambatana na sehemu anayosalia juu yake, bali Kitu anachosalia ndio kimegusana na uchafu huo. yaani hii hua ni sawa na Mtu anaesali juu ya Ardhi safi ambayo imeunganika na ardhi chafu.**'*(Al Mughni)*

MIKONO NA MIGUU KATIKA SUJUD

❖❖❖

Alhamd lillah kua tumemalizanakufakufahamishana kuhusiana na Paji la Uso na Pua Katika Sujud, na tumeona namna inavyotakiwa iwe, Inavyofaa na isivyofaa, Inavyopendekezwa na Inavyokirihisha. Lakini hata hivyo hatujamalizana na Sujud kwani Kulingana na Hadith basi Sujud ni Viungo 7 ambapo kimoja kinahusiana na Paji La Uso na viliyobakia vinahusiana na Mikono na Miguu ambayo hii tutaiangalia kwa vithibitisho na Mitizamo ya Wanazuoni kwa sambamba kuijumuisha yote katika Mada Moja.

Na kama tulivyosema hapo awali kua Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na kipi cha kutanguliza mwanzo chini Unapoelekea katika Sujud, yaani kuna wanaosema kua ni Mikono na kuna wanaosema kua ni Magoti, na Hivyo imekua hakuna Uthibitisho kua kipi ni bora zaid kufika mwanzo chini, hivyo vyovyote hua ni sawa. Na kwa maana hio basi habari hio tunaachana nayo kwa sababu sasa hivi sisi tayari tumeshafika Chini na Paji la Uso na Ncha ya Pua iko chini juu ya Ardhi.

Na Suali lililobakia ni kua Jee Ili Sijda Ihesabike kua ni Sijda jee Mikono yenyewe na Miguu inatakiwa ikae vipi?

Hivyo basi kabla Hatujaendelea zaid basi kwanza tuainishe hali Inavyotakiwa iwe kwa viungo hivyo kwenye Sijda. Na Jambo la kwanza ni kua kuanzia Kiunoni hadi Miguuni basi Uzito wa Mtu Katika hali ya Sijda hua unabebwa na Magoti. Na kuanzia kwenye Kiuno na Mgongo ambao unatakiwa Unyooke hadi Mabegani basi Uzito wake hua unabebwa na Mikono ambayo inatakiwa isiwe ni yenye kushikamana na Mbavu, yaani Mikono inatakiwa iachane na Mbavu huku ikiwa imenyanyuka na hii ni kwa Upande wa Mwanamme.

Ama kwa Upande wa Mwanammke basi Mikono haitakiwi Kuachana na Mbavu kwani kama tulivyosema kua Mwanamke anatakiwa ajikunyate zaidi katika kila hatua Ya Sala yake. Halafu tunapozungumzia Viganja vya Mikono basi Viganja hua vinatakiwa kubeba Uzito wa Mabega kwani Uzito wa Shingo na Kichwa hubebwa na Paji la Uso.

Hivyo katika hali hii basi Viganja hua viko kwenye Usawa wa Mabega karibu na Uso na hivyo vinatakiwa kua ni Vyenye Vidole vilivyoshikamana, na vyenye Kuelekea Upande wa Kibla. Hivyo Vidole vya Mikono havitakiwi kutawanywa kama inavyotakiwa kwenye Rukuu tunapokamata Goti ili kujizuia vizuri zaidi, kwani katika Sijda Vidole vikitawanywa basi vyengine vitaelekea Kibla na Vyengine viyaelekea kulia Ya Kibla na Kushoto ya Kibla.Na visugudi vya Mikono vinatakiwa Kutolala Ardhini yaani isowe kama inavyolala miguu ya mbele Mnyama kama anavyolala Mbwa bali vitakiwa kunyanyuka Juu Ardhini.

Kisha tunapozungumzia kuhusiana na Magoti ambayo imebeba Uzito wa Kutoka Kiunoni Kuja chini basi inatakiwa ihisi uzito huo na hivyo kua ni yenye Kukaa Kiimara. Ardhini ambako hua kunawezekana vizuri zaidi pale Magoti yanapokua hayakushikamana. Yaani inatakiwa iwe kuna Nafasi ya Urefu wa Nyanda Moja baina ya Magoti Mawili.

Na Mtu anapokua katika Hali kama hii ya Sujud basi ili aupate Uimara na Utulivu zaid basi hua Inambidi Kusimamisha Nyao zake na kisha Vidole vyake viwe vimegusa Ardhini huku vidole vyake vya Miguu vikiwa Vimepinda Kuelekea Kibla. Na baada ya kua katika hali kama hii basi ndio Uzito wa Mwili wa Mtu husika utakua umegawika sawia katika Mifupa 7 ya Kusjudia Ardhini.

Hivyo katika kuendelea kwetu mbele zaidi basi kwanza ni lazima turudi tena katika hadith ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* ambayo amesema kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisjudu, basi alikua akigusanisha Pua yake na Paji lake la Uso Ardhini**. **Na alikua alikua si mwenye Kujibana Mikono yake na alikua akiiweka viganja Vyake Sambamba na usawa wa Mabega yak**e'*(At Tirmidhi)*

Na hii ni kwa sababu mbali ya kua Hadith hii imezungumzia kuhusiana na Paji la Uso na Pua katika Kusujudu, lakini pia hadith hii imezungumzia kuhusiana na Mikono katika Sujud.Na amesema Imam At Tirmidhii juu ya hadith hii kua: '**Hadith hii pia imenukuliwa na Abd Allah Ibn *Abbas Radhi Allahu Anhu* na Wail Ibn Hujayr *Radhi Allahu Anhu* na Abu Said Al Khudhry *Radhi Allahu Anhu,* na hii Hadith ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* ni Hadith ambayo ni *Hasan Sahih.'***

Na kwa upande mwengine basi kuna hadith isemayo:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، وَعَمْرٌو النَّاقِدُ، وَزُهَيْرُ بْنُ حَرْبٍ، وَإِسْحَاقُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، - وَاللَّفْظُ لِعَمْرٍو - قَالَ إِسْحَاقُ أَخْبَرَنَا وَقَالَ الآخَرُونَ، حَدَّثَنَا وَكِيعٌ، حَدَّثَنَا جَعْفَرُ بْنُ بُرْقَانَ، عَنْ يَزِيدَ بْنِ الأَصَمِّ، عَنْ مَيْمُونَةَ بِنْتِ الْحَارِثِ، قَالَتْ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم إِذَا سَجَدَ جَافَى حَتَّى يَرَى مَنْ خَلْفَهُ وَضَحَ إِبْطَيْهِ . قَالَ وَكِيعٌ يَعْنِي بَيَاضَهُمَا

Amesema Abu Bakri Ibn Abi Shaybah, kua amesema Amru An Naqidu kua amesmea Zuhayru Ibn Harbi kua amesema Is-haq Ibn Ibrahimkua amesema Is-haqa kua Amesema AL Haruna kua amesema Waqi'i kua amesema Jaffar Ibn Burqana kua amesema Yazid Ibn Assami kua amesema Ummu ul Muuminina Maymuna Bint Harith Al Hilaliye *Radhi Allahu Anha* kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam alipokua Akisujudu, basi alikua akiweka Mikono yake mbali na mwili wake kiasi ya kua Weupe wa Kwapa zake ulikua ukionekana kwa Mtu aliekaa nyuma yak**e.'*(Sahih Muslim)*

Ambapo amesema Shaykh Ul Islami Muhyo Ad Din Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An

Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: '**Maneno ya Hadith hizi yanamaanisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua Akiweka Visugudi vyake na sehemu za Juu za Mikono yake mbali ya Mwili wake.'**

Na amesema Abd Allah Ibn Malik Ibnu Buhainat Al Azdi kua; '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua Akisujudu alikua akitanua Mikono yake kiasi ya kua sisi tulikukua Tuliona Kwapa zake.'***(Imam Al Bukhari)*

Na akasema tena *Ummu Ul Muuminina* Maymuna Bint Harith Al Hilaliye *Radhi Allahu Anha* katika hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ يَحْيَى، وَابْنُ أَبِي عُمَرَ، جَمِيعًا عَنْ سُفْيَانَ، - قَالَ يَحْيَى أَخْبَرَنَا سُفْيَانُ بْنُ عُيَيْنَةَ، - عَنْ عُبَيْدِ اللَّهِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ الأَصَمِّ، عَنْ عَمِّهِ، يَزِيدَ بْنِ الأَصَمِّ عَنْ مَيْمُونَةَ، قَالَتْ كَانَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم إِذَا سَجَدَ لَوْ شَاءَتْ بَهْمَةٌ أَنْ تَمُرَّ بَيْنَ يَدَيْهِ لَمَرَّتْ .

Amesema Yahya Ibn Yahya kua amesema Ibn Abi Umar kua amesema Sufyan kua amesema Yahya kua amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Ubaid Allah Ibn Abd Allahi Al Sami kua amesema Ami yake kua amesema Yazid Ibn Al Sami kua amesema Maymuna *Radhi Allahu Anha:* **'Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua Akisujudu basi alikua Akiziweka sehemu za Juu ya Mikono yake mbali na Mbavu zake kiasi ya kua Kama Kondoo akitaka kupita chini ya Mikono yake basi angeweza kupita'***(Imam Ibn Majah)*

Ambapo anasema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Hua ni Sunna kuziweka mbali na Mwili sehemu za Juu za Mikono na Tumbo kua Mbali kutokana na Mapaja Katika Kusjudu, Kwani amesema Abu Abd Allah (Imam Al Shafii) katika *Al Risala* amesema kua 'Imenukuliwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua Akirukuu basi kama Kondoo hua ni mwenye kuweza Kupita chini ya Mikono yake. Hivyo basi hii inaonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akijitahidi kuinyanyua Mikono yake na Visugudi vyake katika Sijda.'**

Ambapo anasema Imam Ibn Munir kua: '**Hikma ya Kutanua Mikono katika Sijda ni kuonesha kua Kila kiungo kinatakiwa kisimame kwa kujitegemea peke yake na kitofautiane na chenzake kiasi ya kua Mtu atakaposujudu basi hua ni mwenye kuoenakana mwingi na hivyo kila sehemu ya kiungo cha mwili wake kinajitegemea katika Sijida hi**o.'*(Fat-Al Barr)*

Na kuna hadith isemayo kua :**'Qutaybah Ibn Said kua amesema Baqru Ibn Mudhara kua amesema Jafar Ibn Rabiah kua amesema Al A'araj kua amesema Abdi Allahi Ibn Malik Ibn Bukhaynat Al Asdi *Radhi Allahu Anhu* kua:** '**Alikua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati akisujudu akitanua baina ya mikono yake hadi tukawa tunaona Kwapa zake.'**

Kwani pia katika Bukhari na Muslim kuna hadith isemayo:

أَخْبَرَنَا إِسْحَاقُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، قَالَ أَنْبَأَنَا عَبْدَةُ، قَالَ حَدَّثَنَا سَعِيدٌ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ أَنَسٍ، ح وَأَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ مَسْعُودٍ، عَنْ خَالِدٍ، عَنْ شُعْبَةَ، عَنْ قَتَادَةَ، قَالَ سَمِعْتُ أَنَسًا، عَنْ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله

عليه وسلم قَالَ " اعْتَدِلُوا فِي السُّجُودِ وَلاَ يَبْسُطْ أَحَدُكُمْ ذِرَاعَيْهِ انْبِسَاطَ الْكَلْبِ " . اللَّفْظُ لإِسْحَاقَ .

Amesema Is-haq Ibn Ibrahim kua amesema Abdat kua amesema Said kua amesema Qatadah kua amesma Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa *Salam* kua*:*Kuweni wenye hali ya Kati na Kati katika Kusujudu kwenu, na hivyo Asiwe haya Mmoja wenu kua ni mwenye Kutandaza Mikono yake juu ya Ardhi kama atandazavyo Mbwa.'*(*Bukhari na Muslim)*

Na hadith hii ni yenye kuelezea namna inavyotakiwa kua Sijda ya Kila Mmoja wetu miongoni mwetu kwa kuielezea hali hio kwa kutumia maneno ***Aitadilu fii Al Sujud.***

Ambapo anasema Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din Ibn Arabi anatuambia kua**: 'Neno *I'atidal* hua linamaamisha Kuweka sawia Uzito wa Mwili na hivyo kua ni wenye Kuegemea Viungo 7 vya Mwili katika Sujud. Na hivyo Viungo vyote hivyo 7 vya Sujud vya mwili vinabakia kama vilivyo kwenye sehemu zake huku vikiwa ni vyenye kugusa chini Ardhini na kuweza kutofautishwa kaa kuonekana kua hiki kichwa kipo mbele katikati, hii Mikono Nyuma ya Kichwa na viganja vyake baina yake, haya ni Magoti nyuma ya Mikono na hii ni Miguu Nyuma ya Mikono.'**

Ambapo Mkao huu hua ni wenye kuainisha Athari ya uwezo wa Nguvu na Ari ya Kiwiliwili zinazotakiwa kuonekana katika Ibada ya Sala. Na hivyo kuainisha kwa dhahiri namna Viungo hivyo 7 vya Sujud vinavyotekeleza Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kumuabudu pale vinapokua mbele ya Mola wake.

Kwani havitakiwi kuonekana kua vyenye hali ya uregevu na vyenye Uchovu na Uvivu kiasi ya kua Hata visugudi haviwezi kuinuka na vinabakia ardhini na hivyo kuongeza viungo visivyotakiwa katika Sujud.Na ndio maana hali hio ikafananishwa na hali ya Mbwa Mvivu na Aliechoka Taabani.

Kwani anasema Imam Abu Isa Muhammad Ibn Isa Ibn Sawra Ibn Musa Ibn Al Dahhad Ibn Al Sulami Al Tirmidhii kua: '**Kuna Hadith nyingi sana kuhusiana na mada hii kutoka kwa Abd Rahman Ibn Shibli, Jabir, Al Baraa, Abu Humaid, na Aisha *Radhi Allahu Anhum* na zinafanyiwa kazi na Wanazuoni, Ambapo hua inapendekezwa kua na Msimamo wa Kati Katika Sujud na kua inakirihisha Kuitandaza Mikono kama Mbwa wafanyavyo.'**

Na hivyo Miongoni mwa Sunna hua ni kama ilivyosema Hadith ya Abu Humaid Al Saidi *Radhi Allahu Anhu* katika kuielezea Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**'*Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisujdu alikua akiweka viganja vya mikono yake Ardhini bila ya kutanua mikono yake wala kuibana mikono yake.'***(*Sahih Bukhari)*

Ambapo Wanazuoni Wanakubaliana juu ya Uwekaji Visugudi mbali na Mbavu kua ni Sunna inayopendekezwa. Hivyo atakefanya hivyo atalipwa Malipo zaid na asiefanya hivyo hua hafanyi dhambi.

Na hii ni kwa sababu ya hali mbili za Mazingira tofauti zifuatazo: Sababu ya kwanza inatokana na hali ya mazingira ya hali mtu mwenye Kusali peke yake ambapo hua ni vizuri kutanua Mikono lakini tena sio unatakua mikono kama Dege la Kirusi linalobeba Mabomu ya Nyuklia ya Masafa marefu ya Nyuklia na hivyo kila mtu akikuona anaogopa hata kusali karibu nawe. Kwani hata akitaka kusjudu

karibu yako basi kabla kufikisha kichwa chini anakutana na kisugudi chako wewe uliekiwemo kwenye Sijda yako.

Hivyo hii unaweza kufanya unapokua peke yako kwani unaposali Sala ya Jamaa kutanua Mikono hadi ukawakera wenzako hua inakirihisha na kuwakosesha Khushuu wenzako katika Sala. Na hivyo kujikosesha na wewe mwenyewe pia Malipo stahiki ya Ibada yako na kupata Dhambi kwa sababu tu ya kutaka nawe kwapa zako zionekane. Kwani Kulingana na Hadith *ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi ni kua anaewakera Waislam Msikitini basi humkera *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hua ni mwenye kumkera *Allah Subhanah wa Ta'ala.(Imam Ibn Hajar Al Haythami)*

Hivyo ingawa ndio, ni kweli kuna hadith kadhaa zisemazo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitanua mikono yake hadi Weupe wa Kwapa zake ukawa unaonekana. Lakini tusisahau kua Waliokua wakiona Kwapa za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua aidha ni Maamuma na hivyo Wako Nyuma yake na yeye akiwasalisha Sala ya Fardhi .Ama walikua wamekaa Nyuma yake wakimuangalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa anasali Sunna Msikitini au Nyumbani kwake.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakufanya hivyo katika Wakati ambao alikua akisali Nyuma ya Imam pamoja na Waislam wengine, kwa mfano pale alipokua akisalishwa na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu,* kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa Waislam ni Mwenye Huruma.

Na ndio maana katika hili hua ni vizuri zaidi kuifanyia kazi Hadith ya Abu Humayd Al Said *Radhi Allahu Anhu* iliyosema kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alipokua akisujudu alikuaAlikua akiweka Viganja vya mikono yake Ardhini bila Kuitanua mikono yake wala kuibana.**'*(Sahih Bukhari)*

Ama kuhusiana na sababu inayotokana na hali ya Mazingira ya pili ni kua: Mara Nyingi Watu wanapokua Wanasali Sala ya Jamaa, halafu Msikiti ukajaa na kufikia watu kubanana kwenye Safu hua haiwezekani kwa Maamuma kusujudu kwa kuachanisha mikono yao kutokana na Kwapa zao na Mbavu zao kutokana na kujibana huko.Hivyo unakuta Watu wanasujudu wakiwa wamebanana ndani ya Misikiti na mikono yao imeshikamana na Mbavu zao bila ya wao wenyewe kutaka kua katika hali kama hio.Hivyo kama ingekua ni Wajib kutanua Mikono hadi kwapa zionekane basi Jee Sala za Waislam wangapi zingebatilika?

Hivyo tumeona kulingana na Hadith kadhaa ikiwemo ya *Ummu ul Muuminina* Maymuna Bint Haritha Al Hilaliye *Radhi Allahu Anha* ambae ni Mke wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisujudu Alikua akitanua Mikono.Na pia tumeona kulingana na Hadith ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Alikua akiweka Viganja vya mikono yake Ardhini bila Kiitanua mikono yake wala kuibana.

Huku katika hadith zote tunaona kua alikua akihimiza na akionesha Mfano wa kunyanyua Mirfaqayn yaani sehemu za mikono miwili kuanzia viungio vya kiganja hadi kwenye Kisugudi. Na hivyo kukataza kulaza *mirfaqayn* kama wafanyavyo wanyama wanapolala kama Mbwa. n.k

Ambapo hata hivyo kama tulivyosema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliyafanya yote hayo ya kutanua mikono na kuiachanisha na Mbavu zake na hivyo basi kutudhihirishia kua hali zote hizo mbili hua ni Sunna ambayo kila Mtu anaweza kuitekeleza aitakayo lakini kwa kulingana na hali ya Mazingira.

Kwani kama kama ikiwa kutanua Mikono kwako katika Sijda kutamkera aliekua karibu yako basi kihukmu unakua unakirihisha. Na jambo lolote ambalo linaingia katika Hali ya Kukirihisha kihukmu basi kutofanywa kwake hua ni bora zaidi kuliko kulifanya.

Kwa maana hio basi Muhimu zaid kuhusiana Mirfaqayn na Visugudi katika Sujud ni kua Visiwe ni vyenye Kutandazwa na Kugusa Ardhini bali viwe vyenye kunyanyuliwa juu kama inavyoelezea hadith iliyonukuliwa na Imam Muslim Ibn Al Hajjaj ambayo hata hivyo haikusema kuhusiana na Kutanua Mikono ama la, kama inavyotuonesha kwa kusema

Amesema Baraa Ibn Azib *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua:*

اذا سجدث فضع كفيك وارفع مرفقيك

Unaposujudu basi weka Viganja vyako Ardhini na kisha Nyanyua Mirfaqayk yako juu'*(Sahih Muslim)*

na tunapoiangalia hadith hii basi kama tunavyoona kua katika hadith kua ndani yake Mna Amrisho la *Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* kuhusiana na namna Mikono inavyotakiwa iwe katika SujudNa hivyo amrisho linasema kua Weka Viganja Chini na Visugudi vinyanyue.

Na kikanuni kulingana na Sharia za Dini ya Kiislam basi ni kua Ummah wa Kiislam hua hauna budi kufuata Maamrisho bila ya kipingamizi pale inapokua maamrisho hayo yanatoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala, Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Wenye Amri Juu ya Waislam miongoni mwao yaani Wanazuoni.

Kama zilivyosema Aya:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِى ٱلأَمْرِ مِنْكُمْ﴾

YaAyyuha Al Ladhiina Amanuu AtiaAu Allaha, w AtiaAu Al Rasulu wa Uulii Al Amri Minkum.*(Surat An Nisaa 4:59)*

*Tafsir:**Enyi MlioaminiMtiini Allah(Subhanah wa Taala) Na Mtiini Rasul Allah (Salallahu Alayhi wa Salam)NaWenye Amri Miongoni mwenu.***

Na hivyo katika hili la suali la Mirfaqayn basi tunavyotakiwa ni kufuata Amrisho la Hadith hii ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Kwa kunyanyua bila kuwakirihisha wengine.

Ama kwa upande mwengine basi amesema Wail Ibn Hujayr *Radhi Allahu Anhu* kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua kila anaporukuu Hutanua Vidole vyake vya mikono, na kila anaposujudu Huviweka pamoja vidole vyake vya mikono'***(Imam Al Hakim)*

Hivyo mbali ya Kuweka chini Kiganja na Kunyanyua Visugudi lakini pia hadith hii inatudhihirishia Hukmu nyengine ya namna ya inavyotakiwa Mikono iwe kwenye Sujud.

Hivyo mbali ya Kuweka chini Kiganja na Kunyanyua Visugudi lakini pia hadith hii inatudhihirishia Hukmu nyengine yaNamna ya inavyotakiwa Mikono iwe kwenye Sujud.

Kwani amesema pia Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisujudu alikua akielekeza Vidole vyake kuelekea Kibla.'***(Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri)*

Na akasema Imam Abu Al Qasim Abd Qarim Ibn Muhammad Ibn Abd Al Karim Ibn Fadhl Al Rafii Al Qazwini Al Shafii kua: '**Hadith hii ya *Ummu Ul Muuminin* na Aisha *Radhi Allahu Anha* ni Ushahidi kwamba Katika Sujud Inapendekezwa kwa Vidoe vya Mikono yote Miwili Vinyoooshwe na kushikamanishwa Kuelekea Kibla.'**

Na Imam Ibn Hibban anasema kua:

عن وائل بن حجر رضي الله عنه : أن النبي صلى الله عليه وسلم كان إذا ركع فَرَّجَ أصابِعَه وإذا سَجد ضَمَّ أصَابِعه.

'**Amesema Wail Ibn Hujayr *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akitanua Vidole vyake vya Mikono anaporukuu katika Sala na anaposujudu huvibana vidole vyake vya Mikono.'** *(Sunan Ibn Hibban)*

Ambapo maana ya Hadith zoye hizi ziko wazi kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitanua Vidole vyake vye Miguu kwa ajili ya kushika na Kuyaegemea Magoti yake katika Rukuu na alibana vidole vya Mikono yake kunakomuwezesha Kuelekea Kibla kwa Kila kiungo cha Mwili wake kutokana na Viungo Saba vya Sujud.

Kwani amesema Imam Malik Ibn Anas kua Imam Nafii Kua amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mmoja wenu Akisujudu basi hua anaelekea Kibla kwa Mikono yake na kisha Anasujudu kwa Paji lake la Uso.'***(Muwatta Imam Malik)*

Ambapo bila ya shaka haiwezekani Kusjudu bila ya Kutanguliza Mikono kwanza mbali ya kua Mtu umeshapiga Magoti, hivyo baada ya Kupiga Magoti ndio Unatanguliza Mikono iliuobanwa vidole vyake na hivyo viganja na vidole vyake vinaelekea Kibla.

Na kisha ndio Unaweka Paji la Uso Chini Ardhini, na hivyo ndivyo inavyopendekezwa kama alivyosema Al Imam Al Rafii.Na Imam Al Rafii amesema kua inapendekezwa na ndio mtizamo wa Imam Muhamamd Idris Al Shafii pia na kwa upande mwengine basi kuna baadhi ya Wanazuoni wanasema kua hakuna ulazima huo.

Ambapo ḳuhusiana na sehemu inayokaa Mikono katika wakati wa Sijda, basi kuna Tofauti ya Mitizamo pia. Na hii ni kwa sababu ukiangalia vizuri basi utaona kua hii inategemeana na mtizamo wa Mtu juu ya hili kwani kwa mmoja huenda akaona kua Viganja vimekaa pembeni ya Kichwa au Uso na kuna watakaona kua Viganja vimekaa baina ya Mabega mawili hata kama Viganja hivyo Viko katika sehemu moja.

Na hii ni kwa Sababu Mtu anaposujudu ipasavyo basi viganja vitaonekana kua viko katika Usawa wa Mabega na vidole vyake viko kwenye Usawa wa Mwanzoni mwa Uso. Na mifano ya Hadith zinazoelezea Mitizamo miwili hii tofauti ni ile wa Hadith mbili tofauti zisemazo kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ، بُنْدَارٌ حَدَّثَنَا أَبُو عَامِرٍ الْعَقَدِيُّ، حَدَّثَنَا فُلَيْحُ بْنُ سُلَيْمَانَ، حَدَّثَنِي عَبَّاسُ بْنُ سَهْلٍ، عَنْ أَبِي حُمَيْدٍ السَّاعِدِيِّ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم كَانَ إِذَا سَجَدَ أَمْكَنَ أَنْفَهُ وَجَبْهَتَهُ مِنَ الأَرْضِ وَنَحَّى يَدَيْهِ عَنْ جَنْبَيْهِ وَوَضَعَ كَفَّيْهِ حَذْوَ مَنْكِبَيْهِ . قَالَ وَفِي الْبَابِ عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ وَوَائِلِ بْنِ حُجْرٍ وَأَبِي سَعِيدٍ . قَالَ أَبُو عِيسَى حَدِيثُ أَبِي حُمَيْدٍ حَدِيثٌ حَسَنٌ صَحِيحٌ . وَالْعَمَلُ عَلَيْهِ عِنْدَ أَهْلِ الْعِلْمِ أَنْ يَسْجُدَ الرَّجُلُ عَلَى جَبْهَتِهِ وَأَنْفِهِ فَإِنْ سَجَدَ عَلَى جَبْهَتِهِ دُونَ أَنْفِهِ فَقَدْ قَالَ قَوْمٌ مِنْ أَهْلِ الْعِلْمِ يُجْزِئُهُ . وَقَالَ غَيْرُهُمْ لاَ يُجْزِئُهُ حَتَّى يَسْجُدَ عَلَى الْجَبْهَةِ وَالأَنْفِ .

AmesemaMuhamamd Ibn Bashar kua: Amesema Abu Amir Al A'aqadiyu kua Amesema Fulayh Ibn Sulayman kua Amesema Abbas Ibn Sahl kutoka kwa Abu Humayd Al Saadi amesema kua: *Radhi Allahu Anhu kua: '**Wakati Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alipokua akisjudu, basi alikua akigusanisha Pua yake na Paji lake la Uso Ardhini**. **Na alikua alikua si mwenye Kujibana Mikono yake na alikua akiiweka viganja Vyake Sambamba na usawa wa Mabega yak**e.'*(At Tirmidhi)*

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii na kwa upande mwengine basi kuna Hadith isemayo kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*kua: Nimemuona mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akisujudu huku Mikono yake ikiwa pembeni ya Masikio yake***(Imam Abu Daud)*

Ambapo aina hii ya uwekaji wa Mikono wa Hadith hii umetajwa tena na Imam Said Ibn Jubayr.Hivyo Ukamililifu wa Viganja vya Mikono katika Sujud hua ni Kuyalaza matumbo ya MikonoSambamba baina ya Mabega ama kukaribia Masikio.

Lakini kufanya vyenginevyo hua hakubatilishi Sala, yaani kwa mfano pia plae inapotokea kua Safu zimejaa na watu wamebanana na hivyo katika Kusjudu hua wamejibana na inakua vigumu kuweka Viganja katika sehemu zilizotajwa kwenye Hadith na hivyo badala yake mtu hua ni mwenye kuweza kufikisha Ncha za Vidole vyake katika usawa wa mabega tu na si zaidi katika kuweka Viganja vyake chini.

Kwani amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Kama ikiwa Mtu atasujudu kwa kufanikiwa kuweka Sehemu ya Viganja vyake kama vile awezavyo kuweka Paji la Uso basi hii hua inatosheleza.'**Hivyo kuhusiana na Mikono katika Sijda basi Muhimu ni kua Imetumiwa katika Sujud husika kwa Viganja kugusishwa Ardhini huku Visugudi vikiwa si vyenye kugusa Ardhi bali viko juu.

Tunarudi tena katika Hadith ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* kwa sababu hii ndio hadith ambayo imenukuliwa sana na Wanazuoni pale tunapozungumzia kuhusiana na Ibada ya Sala ambapo Hadith hii inasema kwamba: '**Kutoka kwa Muhammad Ibn Amr Ibn Ataa kua: Wakati Abu Humayd Al Saadi akiwa amekaa na Masahaba Takriban *10 Radhi Allahu Anhum* Akiwemo Abu Qatadah**. **Basi Abu Humayd akasema kuwaambia Masahaba hao *Radhi Allahu Anhum* kua: 'Hakika mimi ndie Mjuzi zaidi Miongoni mwenu Kuhusiana na Namna alivyokua Akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakashangaa na kusema: Kwanini? Wakati wewe hukumfuata zaidi ya tulivyokua Tukimfuata sisi na wala hukufauatana nae Kabla yetu.'

Abu Humayd akasema: 'Mimi nasema kua Hakika Mimi ndie Nnaejua zaidi.'

Masahaba wakasema: 'Haya sawa,hivyo Hebu Tuoneshe hivyo unavyojua wewe.'

Abu Humayd Al Saadi akasema: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anaposimama Kusali basi alikua ananyanyua Mikono yake sawia na Mabega yake. Huku akisema Takbir, Kisha hua anasubiri hadi kila Mfupa wa sehemu ya Mwili wake uwe Umetulia sawasawa. kisha anaanza kusoma Qur'an, na kisha ananyanyua Mikono yake sawia na Mabega yake na Kusema Takbir na Kurukuu huku akiweka viganja vyake kwenye Magoti yake. Kisha alikua akisimama wima huku kichwa chake kikiwa hakikuinama sana wala hakijainuka sana na kusema *Sami Allahu Liman Hamida.'*

Kisha Huinua Mikono yake hadi Usawa wa Mabega huku akisimama wima. Huku mikono yake ikiwa pembeni mwake. Kisha husema Allahu Akbar huku akielekea Chini Ardhini akisjudu na kugusisha Paji lake la Uso na Pua yake Ardhini na kuweka viganja vya mikono ya yake Ardhini bila ya kuitanua sana mikono yake wala kuibana sana na alikua akiviweka Viganja sambamba na usawa wa mabega yake. Na katika Kusujdu alikua hayakutanishi Mapaja yake pamoja na alikua akikunja vidole vyake vya miguu kuelekea Kibla.

Kisha Anaponyanyuka kutoka kwenye Sijda husema Allahu Akbar na kukaa kitako kwa kuunyoosha Mguu wake wa Kushoto na kuukalia juu yake, mguu wa kulia ukiwa umeelekea Kibla vidole vyake na hukaa katika hali hio hadi Mifupa yake Ikatulia. Kisha Husema Allahu Akbar na Kuajudu tena kama mwanzo,na kisha hunyanyuka tenana kuja Kusimama, Kisha anafanya tena katika Rakaa ya pili kama alivyofanya kwenye Rakaa ya kwanza na kukaa Attahiyat.

Na kisha husema Allahu Akbar na kusimama huku akiwa mwenye kunyanyua Mikono yake hadi Mabegani na kisha kuifunga kama alivyofana katika Tabkir ya Mwanzo ya Kuingia kwenye Sala.*Rasul Allah salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali hivyo hivyo na akifika katika Sijda inayofuatiwa na Sujud basi anapoka kitako basi huusogeza kulia Mguu wake wa Kushoto na kuweka kalio lake la Kushoto Juu ya Ardhi.Masahaba wakasema Umesema kweli, kwani hivyo ndivyo alivyokua akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam**(****Imam Abu Daud, Imam Bukhari, Imam At Tirmidhii)***

Hivyo tumeona katika Hadith ya Imam Abu Daud inayoelezea kuhusiana na Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutoka kwa Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua Akisujdu basi Alikua akitanua Mapaja yake na hayakutanishi Kwa maana hio basi hii inaonesha kua kwa Ujumla alikua haiweka pamoja Miguu yake kuanzia Magotini, Mapajani hadi kwenye Nyayo na vidole vya Miguu.'**

Ambapo kutokana na Hadith hii ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* basi ndio Wanazuoni wamehitimisha kwa kukubaliana kua: '**Inapendekezwa Kuachanisha Miguu Katika Sala.'**

Ambapo kama tulipoona hapo kabla kua Kulingana na Madhab ya Imam Abu Hanifa basi hua. '**Inapendekezwa kuacha Nafasi Japo yenye Upana wa Vidole Vinne vya Mkono.Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Japo Nyanda Moja.'**

‘Na kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema Inapendekezwa iwachwe nafasi ya Kati na Kati isiwe kubwa sana wala isiwe ndogo sana’*(Al Fiqh Ul Islam)*

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: ‘**Al Shafii na As-hab Al Wujuh wamesema kua Inapendekezwa kwa Mtu anaesujudu kutenganisha Magoti yake na pia Miguu yake**. **Na Al Qadhi Abu Tayyib Al Tabari amesema Katika Ufafanuzi wake kua : Wanazuoni wenzetu wamesema kua Inatakiwa iwe kuna sehemu ya masafa ya Nyanda Moja baina ya Miguu miwi**li.’*(Al Majmuu)*

Na kwa upande mwengine basi kuna Hadith isemayo kua:

قالت عائشةُ زَوجُ النَّبيِّ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ : فقدتُ رسولَ اللَّهِ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ وَكانَ معي علَى فراشي فوجدتُه ساجدًا راصًّا عقِبَيهِ مُستقبِلًا بأطرافِ أصابعِه القِبلَةَ فسمِعتُه يقولُ : أعوذُ برِضاكَ مِن سخطِك وبعفْوِك مِن عقوبتِك وبِكَ مِنكَ أُثني علَيكَ لا أبلغُ كلَّ ما فيكَ قالت : فلمَّا انصرفَ قال : يا عائشةُ أخذَكِ شَيطانُكِ فقلتُ : أما لَك شَيطانٌ ؟ قال : ما مِن آدميٍّ إلَّا لَه شيطانٌ ، فقلتُ : يا رسولَ اللَّهِ وأنتَ ؟ قال : وأنا ولَكنِّي دعَوتُ اللَّهَ فَأعانَني علَيهِ فأسلَمَ

Amesema Ummu ul Muuminina Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: ‘**Mimi niligundua kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hayuko pamoja nami Kitandani. Lakini nikamuona akiwa anasujudu huku Visigino vyake vikiwa pamoja na ncha za Vidole vyake vya Miguu vikiwa vimeelekea KiblaNikamsikia akisema: Najikinga Kutokana na Radhi zako dhidi ya Hasira zako, na Nakijikinga kutokana na Usamehevu wako Dhidi ya Adhabu zako na mimi ni mwenye kutoka Kwako na kwako ndio Marudio yangu Nakusifu na Nakutukuza na siwezi Kukutukuza kama Ipasavyo.’ na alipomaliza Kusali akasema: ‘Amekumiliki Shaytani wako?.’**

‘Hakuna IbnAdam isipokua an Shaytani wake’

Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema: ‘Ya Rasul Allah! Hata wewe pia?’ *Rasul Allah Salalllahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Naam Hata mimi pia,ila nilimuomba *Allah Subhanah wa Ta’ala* nikamzidi nguvu na akasilimu.’ *(Imam Ibn Khuzaymah, Imam Ibn Al Mundhir, Imam Ibn Hibban, Imam Al Hakim, Imam Al Bayhaqi, Ibn Abd Al Barr na Imam At Tahawi)*

Ambapo Imam Al Hafidh Al Hakim Al Tirmidhii amesema kuhusiana na Hadith hii kua: ‘**Ingawa Hii ni Hadith Sahih Kulingana na Vigezo vya Shaykhani (yaani Imam Bukhari na Imam Muslim) lakini wao hawakuinukuu Hadith hii, Nami Sijui Hadith nyengine yeyote yenye kutaja kuhusiana na Kubana visigino Katika Sijda isipokua Hadith hii.’**

Na Imam Al Hafidh Shams Ad Din Abu Abdillahi Muhammad Ibn Ahmad Ibn Uthman Ibn Qaymaz Ibn Abdillahi Ibn Turkman Al Fariqi Al Dimash Adh Dhahabi Al Shafii amesema kua: ‘**Hadith hii inazo sifa za Usahihi kulingana na Vigezo vya Imam Bukhari na Muslim.’**

Na Imam Al Faqih Al Hafidh Siraj Ad Din Abu Hafs Ali Ibn Ahmad Ibn Al Mulaqiin Al Shafii Al Misri basi yeye amesema kua**: ‘Sanad ya Hadith hii ni Sahih.’***(Badr Al Munir)*

Hivyo ingawa hizi ni Hadith mbili zenye Mitizamo tofauti, na hivyo anasema Imam An Nawawi katima Sharh Muhadhdhab kua: '**Imam Al Shafii amependekeza jua katika wakati wa Kusujudu basi Mtu asigusanishe Magoti yake wala Miguu yake.'**

Na Al Qadhi Ahu Tayyib Al Tabari Al Shafii akasema katika Al Ta'aliq pia ku**a: As-hab Al Wujuh wetu wamekubaliana kua Miguu katika Sala itanuliwe kwa Upana wa Nyanda moj**a.'

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Shawqani Al Hanbali basi yeye amesema kuhusiana na Hadith ya Abu Humayd Radhi Allahu Anhu kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitenganisha Mapaja yake katika Kusujudu.'***(Nayl Al Awtar)*

Na kwa upande wa Al Muhaqqiq Imam Ibn Aabidin Al Shami Al Hanafi basi yeye anasema kuhusiana na Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: 'I**napendekezwa kwa Miguu kua Pamoja katika wakati wa Kusjudu.'**(*Fatawa Al Mahmudiyya)*

Na kwa upande wa Imam Abu Jafar At Tahawi Al Hanafi basi anasema katika Maani Al Athar kua: '***Ilsaaq* (Kufunga miguu) hakuhusiana kabisa na sharia za Sala, iwe katika kusimama, kurukuu au kusujudu kwa Mwanamme na *Tajaafi* -Kutogusanisha Miguu katika Kisimamo, katika Rukuu na katika Sujud katika Sala kwa Wanaume ni jambo ambalo linajulikana kama *Mashruu* (Lililothibitishwa Kisharia) kwani tumeona kulingana na Sunnah kua wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi Salam*Alikua katika *Tajaafi* (kutawanya Miguu) katika Kurukuu na kusjudu. Na Umma wa Kiislam umefikia Makubaliano ya Ijmaa juu ya Jambo hili.'**

Nahivyo basi kulingana na Vithibitiaho tunaona kua kwa Mwanamme hua inapendekwezwa kutanua miguu katika Kisimamo cha Sala, katika Rukuu na Katika Sujud pia.Na tunaposema kua inapendekezwa basi hua haimaanishi kua ni lazima bali inamaanisha kua ni bora zaid, Na hivyo kutekeleza kwake hua kuna Malipo zaid ambayo kukosekana pale isipotekelezwa.

Ambapo hio ni kwa upande wa Wanaume na kwa Upande wa Wanawake basi kwao wao ni kama tulivyoelezea hapo kabla kua hawatakiwi kutanua miguu katika Sala, kwani kufanya hivyo hua ni Kuringa na Kujiona na wala si kuonesha Unyenyekevu kutokana na Maumbile yao.Hivyo Wanawake wanatakiwa wajibane bane na kujikunyata katika Kisimamo, katika Rukuu na katika Sujud pia.

Kama anavyosema Imam Abu Hanifa Nu'man Ibn Thabit kua: **'Mwanamke anatakiwa akijuksanye katika wakati anaposujudu, anatakiwa aliambatanishe pamoja Tumbo lake na Mapaja yake, kwani njia hii ndio inayomfanya awe emejihifadhi zaidi '***(Al Hidayah)*

Na anasema Imam Malik Ibn Anas kua: **'Mwanamme hutanua Magoti yake, Visugudi vyake na Mapaja huyaweka mbali na Tumbo lake katika wakati wa Kusujudu, ambapo Mwanamke anatakiwa avikusanye viungo vyote hivi vyote pamoja.'***(Al Sharhul Saghir)*

Na anasema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '***Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wametuonesha njia ambayo Wanawake wanatakiwa kujisitiri, na Mimi napendelea kwa Mwanammke kua akiunganishe kila kiungo cha mwili wake na kiungo chengine katika Sijda yake ndani ya Sala, kama vile ambavyo anavyotakiwa kufanya katika Kisimamo chake na Rukuu yake, na Mwanamke anatakiwa kuziweka nguo zake katika hali ya kutobanana na hivyo zinatakiwa kua huru kiupana pana ili Mwili wake usiwe ni wenye kujionesha'***(Kitab Al Umm)***

Na anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: **'Mwanamke hatakiwiki kujitanua katika wakati anaposujudu ndani ya Sala, na hii ni kwa sababu wao wameamrishwa kujihifadh na kujisitiri na hivyo wanatakiwa kuvikusanya pamoja viungo vya miili yao katika Sujud, na wagusanishe Miguu yao wanaposujudu'***(Al Mughni, Imam Ibn Qudamah)*

Hivyo Wanazuoni wanakubaliana kua haipendekezwi kwa Mwanamme kufanya *Ilsaaq* (Kubana Miguu) Katika hatua zote za Sala ikiwemo katika Kusimama, Kurukuu, Kusujudu ndani yake. Isipokua kwa Mwanamke kufanya *Ilsaaq* hua inapendekezwapia Wanakubaliana kua Kufanya *Tajaafa* (Kutanua kidogo Miguu kwa kiasi fulani) Kunapendekezwa kwa Wanaume katika Sala pale wanapokua katika hatua za Kusimama,Kurukuu na KusujuduAmbapo kwa Wanawake hua haipendekezwi Kabisa kufanya *Tajaafa* na hua inakirihisha kutokana na Maumbile yao.

Na hivyo tukirudi tena katika Hadith isemayo kua: '**Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: Mimi niligundua kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hayuko pamoja nami Kitandani Lakini nikamuona akiwa anasujudu huku Visigino vyake vikiwa pamoja na ncha za Vidole vyake vya Miguu vikiwa vimeelekea Kibla.'***(Imam Ibn Khuzaymah)*

basi tunaona kua ingawa hadith hii haitiliwi maanani sana kuhusiana kwa sababu inazungumzia kuhusiana na *Ilsaaq* lakini kwa upande mwengine basi tunaona kua hii ni miongoni mwa Hadith inayotumika pia katika kuainisha kuhusiana na namna inavyotakiwa vidole vya Miguu vikae vipi katika Sijda.

Ambapo ndani yake Hadith hii tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhiwa Salam* Alikua ameelekeza Vidole vyake vya Miguu katika Upande wa Kibla. Hivyo hadith hii ya *Aisha Radhi Allahu Anha* hua inatumika kuiunga mkono na kuupa nguvu uthibitisho wa hoja iliyomo kwenye Hadith ya Abu Humayd Al *Saadi Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pale aliposema kua:

'Na katika Kusujdu kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi alikua hayakutanishi Mapaja yake pamoja na alikua akikunja vidole vyake vya miguu kuelekea Kibla. **Kisha Anaponyanyuka kutoka kwenye Sijda husema *Allahu Akbar* na kukaa kitako kwa kwa kuunyoosha Mguu wake wa Kushoto na kuukalia juu yake, mguu wa kulia ukiwa umeelekea Kibla vidole vyake na hukaa katika hali hio hadi Mifupa yake *Ikatulia.'****(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhi)*

Hivyo kutokana na vithibitisho vya Hadith mbili hizi Sahih na nyenginezo zinazobebana kihoja basi tunaona kua kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua: '**Kukunja Vidole vya Miguu na kuvielekeza Kibla katika wakati wa Sijda Ni sehemu kuu ya Sifa ya Ukamilifu wa Sijda**. **Ambapo Mtu anatakiwa Vidole avikunje Japo kidogo vielekee Kibla na kama hakuvikunja basi Sijda yake hio hua ni Batili,na hivyo kuifanya Sala pia kua ni Batili.'**

Ambapo huo ndio Mtizamo unaojulikana kama *Al Qawl Al Mutammad* yaani ndio Mtizamo Unategemewa katika Madhhab ya Imam Al Shafii.

Kwani anasema Al Khatib Al Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shirbini Al Shafii kua: '**Watu wanaposujudu basi sehemu zao za Ndani(Nyayo) za Vidole vya Miguu yao zinatakiwa ziguse chiniArdhini, na hii ni kwa sababu si Ncha za Vidole hivyo wala sehemu za Juu za vidole hivyo vya Miguu vitakavyoweza kutosheleza katika hilo.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Na bila ya shaka ili miguu ya Mtu anaesali iwe ni yenye kuelekea Kibla katika Kusujudu basi inabidi sehemu zake za chini ya Vidole ziwe ni zenye kugusa Ardhini na hapo ndipo vidole vitakapoelekea Kibla.

Ambapo amesema alivyofafanua Imam Al Khatib Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shibrini kua: '**Hua Inatosheleza Kugusisha chini Ardhini Kila Moja kati ya sehemu 7 za viungo vya Sujud kama vile linavyowekwa Paji la Uso.'**

Kwani kwa upande mwengine basi tunaona kua pia kuna Mtizamo usemao kua: '**Kunyoosha Vidole Vya Miguu kuelekea Kibla hua ni Sunna na wala Si Wajib'** Ambapo mtizamo huu ni wenye kupingaa na Mtizamo unaotegemewa katika Madhhab ya Imam Al Shafi.

Na hili tunaliona kwenye Mitizamo ya Madhhab mengineyo kwa mfano anasema Khatimat Al Muhaqiqin wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ambae ni Imam Mansur Ibn Yunus Al Buhuti Al Hanbali ambae yeye anasema kua: '**Inatosheleza kwa Mtu mwenye Kusujudu kua ni mwenye Kugusisha Ardhini Viungo Saba vya Mwili, hata kwa kutumia sehemu ya Nyuma ya Viganja kwa Mikono au sehemu ya Juu ya Miguu kwa Miguu, kama kwamba anasujudu kwa Ncha za Vidole vya Mikono au ncha za Vidole vya Miguu, na hii ni kutokana na maana iliyowazi ya Hadith Kwa sababu Muhimu ni kugusisha Paji la Uso,Mikono na Miguu'***(Kashaaf Al Qinaa)*

Ambapo kwa Upande Al Muhaqiq wa Madhhab Ya Imam Abu Hanifa yaani Imam Ibn Abidin Al Shami basi yeye anasema kua: '**Ni Wajibu katika Wakati wa Kusujdu kugusisha chini sehemu yeyote ile ya Mguu au Kidole japo kwa mda mchache.'***(Radd Al Mukhtar)*

Na kwa upande wa Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Muhammad At Tarabulsi Al Hattab Al Ruyani Al Maliki ambae ni maarufu kama Imam Al Hattab Al Saghir anasema katika Kitabu chake kinachotegemewa katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Malik kiitwacho kua: '**Hakuna Sharti katika Nguzo ya Kusujud Muhimu ni kua Mtu umegisisha Ardhini Viungo 7 vya Sujud**.'*(Mawahib Al Jalil)*

Hivyo tunapoangalia zaidi kuhusiana na Sehemu saba za Vingo vya mwili vya Kusujudia basi tunaona kua Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii anasema kua: '**Kugusisha Ardhini Viungo Saba vya Kusujudia hua ni Wajibu katika Madhhab yetu.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Sulayman Ibn Muhammad Al Bujaraymi Al Shafii basi katika Kufafanua kuhusiana na Kauli ya Imam Al Khatib Al Shirbini kuhusiana na hali ya Vidole katika Sijda basi anasema: '**Vidole vinahesabika katika viungo hivyo Saba, vya Sujud japo kwa sehemu ya Kidole Japo Kimoja kwa Kila Mguu.'***(Hashiya Al Bujaraymi)*

Na kutokana na Mtizamo huu wa Imam Al Bujaraymi basi tunaona kwa upande mwengine tunaona kua katika Madhhab ya Imam Al Shafii kuna Mtizamo mwengine pia unaoonesha kua Kupinda Vidole Kuvielekezea Kibla hua ni Sunnah na hivyo Kutovipindisha Vidole vya Miguu hua Hakubatilishi Sijda,kwa Sababu sio Wajib bali ni Sunnah.

Ambapo Mtizamo huu hua ni Mtizamo Usiokua Mashhuri, yaani Usiotumika kutokana na Kutokukubalika sana na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii. Mbali ya Kua huu ndio Mtizamo wa Madhhab mengine kama tulivyosema hapo kabla.

Kwani kwa upande wa Imam Ibn Abidin Al Shami Al Hanafi basi yeye anasema kua: '**Hua ni Fardhi Kugusisha Ardhini Japo Kidole Kimoja cha Kila Mguu katika Wakati wa Kusjudu japo kwa**

Muda mfupi. **Kwani Inakirihisha Kutoweka Vidole vya Mguu kwa Kuunyanyua Mguu bila ya kua na Sababu inaoruhusika Kisharia.'***(Radd Al Mukhtar)*

Kwa maana hio basi Wanazuoni wa Madhhab mengine Wanakubaliana kua Kugusisha Vidole vya Miguu Ardhini na Kuvipindisha Kuelekea Kibla hua ni Sunna Iliyothibitishwa. Na hii ni kulingana na njia Wanazozitumia katika Kutoa Hukmu katika Vyanzo vya Sharia za Dini ya Kiislam, na hivyo kwao wao basi Kutopindisha Vidole hua Hakubatilishi Sijda.

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii mbali ya kua Mtizamo huo pia upo lakini katika Hili basi kuna Qawlayni (Kauli Mbili) na hivyo Matizamo wenye Nguvu zaid hua ni kua Kutofanya hivyo hua kunabatilisha Sijda na hivyo Kubatilisha Sala pia.

Hivyo tunaona kua Kulingana na Hadith basi ni kua Ni Sunna katika Wakati wa Kusujudu kuvipinda vidole vya Miguu ili navyo vielekee Kibla.Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Kukunja Vidole vya Miguu kuelekea Kibla hua ni Wajib.

Ambapo Mtizamo huu wa Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii Unatuonesha namna Wanazuoni wake walivyokua wako katika Mstari wa Mbele katika Kusimamia Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Kwani Imam Muhammad Idris Al Shafii Mwenyewe alikua na Sifa ya kua ni Mtu mwenye Kusimamia Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ipasavyo.

Na hili tumeliona wazi wazi katika sehemu kadhaa katika kuangalia kwetu na kufahamishana kuhusiana na Sujud katika Uislam na aina zake hususan Sujud ya Ndani ya Ibada ya Sala.Ambayo ndio kitu ambacho kimetupelekea kuiangalia Ibada ya Sala ili tupate kuijua vizuri kulingana na mitizamo ya Madhhab tofauti.Ambapo katika kila hatua ya Sala basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wamekua ni wenye Sifa ya Ansar Sunnah katika Ibada ya Sala.

Na hili litathibitishwa zaidi katika kila hatua tunayoendelea nayo hadi mwisho wa Kitabu chetu hiki.Kwani hali imekua ni Tofauti na wale ambao leo hii ndio wanajiita kua ni Ansar Sunnah au Salafi ambao Asili yao ni katika Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Na unapofuatilia kwa kina basi Unaona kua wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wa karibuni wakiwemo kina Marhum Shaykh Al Uthaymin na Shaykh Ibn Baaz wamekua ni wenye kuachana na Mitizamo mingi sana ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Ahmad Ibm Hanbal na hivyo kua ni wenye kuelemea kwenye Mitizamo ya Imam Muhammad Idris Al Shafii.

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Ibada ya Sala katika hatua ya Kusujudu na Sunna na Wajibu wa Kukunja Vidole na Kuvielekeza Kibla, basi kuna Suali Moja ambalo hua linajitokeza . Na Suali hili linahusiana na Wale wanaosali wakiwa Wamevaa Viatu katika Miskiti ambao Wanajiita kua ni Ansari Sunnah.

Na ingawa sitaki hapa kuzungumzia kuhusiana na Viatu Msikitini kwa sababu hatujafikia wakati wake, kwani tutaizungumzia itakapofikia wakati wa kuzungumzia kuhusiana na Mavazi yanayoruhusika na yasiyoruhusika katika Sala, katika kurasa za mbele za Kitaub hiki.Inshaa Allah.

Lakini Sasa Suali la Kujiuliza kuhusiana na hawa Wanaosali na Viatu Msikitini ni kua:**Sawa Ni kweli Kuna Hadith zisemazo kua *Rasul Allah Salallaju Alayhi wa Salam* alisali na Viatu.**

Ila Jee wanajua ilikua katika Mazingira gani?

Na jee Mazingira yetu ya Leo yanaruhusu Mtu Kusali na Viatu hadi Misikitini?

Na Jee ni aina Gani ya Viatu Alivyokua Amevaa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Wakati huo?

Na jee Viatu hivyo ndio Kama Viatu vyetu vya leo?

Na Jee kulingana na Viatu vyetu vya Leo Ukisali Navyo Utaweza Kuipata Sunna ya Kupindisha Vidole na kuelekeza Kibla?

Na kama ikiwa Vidole haviwezi kupinda na kuelekea Kibla kwa Sababu ya Kiatu ambacho Hakifanani na Kiatu cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* cha wakati huo basi Jee hii inakua ni Kufuata Sunna Na Kuinusuru au inakua ni kufuata Matamanio ya Nafsi na Kuyakumbatia tu Katika Ibada?

Amesema Abu Abd Allah Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* amesema kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaongoza Masahaba zake katika Sala na kisha Akakaa Pamoja nao baadhi yao miongoni mwao.**

Na Mara akaingia Mtu akaanza Kusali, lakini Hatua zake zilikua ni za Haraka sana kama Kuku anaedonoa donoa.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua; Mmemuona Mtu Huyu?**

Kwani Mtu yeyote atakaekufa wakati akiwa Anafanya kama hivi basi atakua si mwenye Kufariki katika Dini ya Muhammad. Kwani Sala yake inafanana na Kunguru anaedonoa Damu. Mtu Anaerukuu na Kisha Akadonoa kwenye Sijda yake basi hua ni Kama Mtu Mwenye Njaa na Kisha akawa si mwenye Kula zaidi ya Tende Moja au Mbili. Jee Itamsaidia Nini' *(Sahih Ibn Khuzaymah)*

وَعَنْ أَبِي قَتَادَةَ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «أَسْوَأُ النَّاسِ سَرِقَةً الَّذِي يَسْرِقُ مِنْ صَلَاتِهِ» . قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ وَكَيْفَ يَسْرِقُ مِنْ صَلَاتِهِ؟ قَالَ: لَا يتم ركوعها وَلَا سجودها ". رَوَاهُ أَحْمد

Na amesema Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*amesema kua Mwizi Mbaya zaidi ni Yule anaejiibia kutoka katika Sala yake'**.

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakauliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah! Hivi itakuaje hadi Mtu awe ni mwenye Kujiibia kutoka katika Sala yake?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: Kwa Kutokamilisha Rukuu zake wala Sujudu zake(*Sahih Ibn Khuzaymah*)

Ambapo Hadith hii pia imenukuliwa na Imam Al Tabarani, Imam Al Hakim ambao wamesema kua Hadith hii ni Sahih kulingana na Vigezo vya Imam Bukhari na Muslim.

Ambapo kwa upande wa Al Faqih, Imam Al Muhaqiqin Imam Shuhab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Walionukuu Hadith hii ni wenye kuaminika kwa usahih'**

Hivyo nasi tunaakumbushana kuhusiana na Sujud na aina zake Katika Uislam na tunaangalia kuhusiana na Sujud ya Ndani ya Sala.Ambapo Hadith mbili hizi zinatuonesha umuhimu wa kua na Utulivu katika Sujud baada ya kua tayari umeshatimiza Masharti yanayotakikana katika Sujud. Yaani kugusisha Viungo vyote 7 vya Sujud Ardhini.

Ambapo Hadith zinatuonesha pia kua Haiwezekani kupata Mafanikio yanayatakiwa kwenye Sujud bila ya kua na Utulivu ndani yake.Na hivyo kutuwekea wazi kua Utulivu wako katika Rukuu na Sujud hukupelekea kua niwenye kufuzu moja kwa Moja, hata kabla ya kufanya Dhikr zinazotakiwa kutamkwa ndani yake.

Na hivyo kutuwekea wazi kua Utulivu wako katika Rukuu na Sujud hukupelekea kua niwenye kufuzu moja kwa Moja, hata kabla ya kufanya Dhikr zinazotakiwa kutamkwa ndani yake na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza jambo la udonoaji kwenye Sujud kama zinavyosema Haidth kua:

حَدَّثَنَا أَبُو الْوَلِيدِ الطَّيَالِسِيُّ، حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، عَنْ يَزِيدَ بْنِ أَبِي حَبِيبٍ، عَنْ جَعْفَرِ بْنِ الْحَكَمِ، ح وَحَدَّثَنَا قُتَيْبَةُ، حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، عَنْ جَعْفَرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ الأَنْصَارِيِّ، عَنْ تَمِيمِ بْنِ مَحْمُودٍ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ شِبْلٍ، قَالَ نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَنْ نَقْرَةِ الْغُرَابِ وَافْتِرَاشِ السَّبُعِ وَأَنْ يُوَطِّنَ الرَّجُلُ الْمَكَانَ فِي الْمَسْجِدِ كَمَا يُوَطِّنُ الْبَعِيرُ . هَذَا لَفْظُ قُتَيْبَةَ.

Amesema Abu Walid Al Tayalisi kua amesema Al Layth kua amesema Yazid Ibn Abi Habib kua amesema Jaffar Ibn Hakim kua amesema Qutaybah kua amesema Layth kua amesema Jafar Ibn Abd Allah Al Ansari kua amesema Tamim Ibn Mahmud kua amesema Abd Rahman Ibn Shibli*Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza katika Sala Kudonoa Kama Kunguru, Kulaza Mikono kama Mnyama wa Mwituni na Kuchagua Sehemu Maalum Msikitini kama vile Ngamia Anavyochagua sehemu zizini(Sunan Ibn Majah)Hii ni Hasan Hadith ambayo imenukuliwa na Imam Ahmad na Abu Daud pia.

Na inatuonesha Mambo ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameyakataza katika Sala na tunapoingia Misikiti.Kwani amekataza Kudonoa Donoa kama Kunguru au Kuku anavyodonoa Mtama, kwenye Sijda yaani Kufupisha Sijda. Bali Mtu Unatakiwa Kutulia unapokua Ndani ya Sijda hadi aupate utulivu.Kwa sababu Kudonoa Donoa kwenye Sijda hua si Kufupisha Sujud tu, bali hua ni Kufupisha Sala yenyewe yote kwa Ujumla.Na hakuna afanyae hivyo isipokua hua ni Mnafiq.

Kwani anasema Imam At Tirmidhii katika hadith ifuatayo kua:

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ حُجْرٍ، حَدَّثَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ جَعْفَرٍ، عَنِ الْعَلاَءِ بْنِ عَبْدِ الرَّحْمَنِ، أَنَّهُ دَخَلَ عَلَى أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ فِي دَارِهِ بِالْبَصْرَةِ حِينَ انْصَرَفَ مِنَ الظُّهْرِ وَدَارُهُ بِجَنْبِ الْمَسْجِدِ فَقَالَ قُومُوا فَصَلُّوا الْعَصْرَ . قَالَ فَقُمْنَا فَصَلَّيْنَا فَلَمَّا انْصَرَفْنَا قَالَ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَقُولُ " تِلْكَ صَلاَةُ الْمُنَافِقِ

يَجْلِسُ يَرْقُبُ الشَّمْسَ حَتَّى إِذَا كَانَتْ بَيْنَ قَرْنَىِ الشَّيْطَانِ قَامَ فَنَقَرَ أَرْبَعًا لاَ يَذْكُرُ اللَّهَ فِيهَا إِلاَّ قَلِيلاً " .

قَالَ أَبُو عِيسَى هَذَا حَدِيثٌ حَسَنٌ صَحِيحٌ .

Amesema Aliyu Ibn Hujri kua amesema Ismail Ibn Jaffar kua Amesema Alaa Ibn Abd Rahman kua: Nilimtembelea Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* Nyumbani kwake katika Ardhi ya Basra baada ya kumaliza Salat Al Dhuhr. **Na nyumba yake ilikua pembeni ya Msikiti. Hivyo akasema: Nyanyuka kwa ajili ya Kusali Al Asr**. **Hivyo Tukanyanyuka na kusali Al Asr, na baada ya kumaliza basi Anas akasema:Mimi nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akisema kua: Hua ni Sala ya Mnafiq ile ambayo Mtu hua anakaa na Kusubiri Hadi Jua liwe baina ya Pembe mbili za Shaytan, na kisha ndio anasimama na Kudonoa donoa Rakaa zake nne bila ya Kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yak**e*(Imam At Tirmidhii)*

Naam..hivyo Kudonoa katika Sala imekatazwa, kwa sababu hukosekana Utulivu na Dhikr Allah ndani ya Sala.

Kisha Hadith yetu ya Qutaibah iiliyokataza Mambo Matatu, basi imekataza Kutandaza Mikono katika Wakati wa Kusujudu kama wafanyavyo Wanyama wa Mwituni.Na kisha pia Hadith ikakataza kwa Mtu kua ni Mwenye Kuchagua sehemu Maalum Msikitini na hivyo hio ndio hua sehemu yake hivyo lazima kila siku asali katika sehemu hio hio.

ADHKAR ZA SUJUD

❖❖❖

Neno a'Ala kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kua Juu Zaidi, Kupanda, Kutukuka, Kuzidi, Kupanda Daraja zaidi, Kupanda Heshima Zaidi,Kushinda Zaidi.

Neno aAla ndio Lililotoa neno Ta'ala ambalo hua linamaanisha Kua Juu Zaidi kwa Umbali Mkubwa Sana na Ukibwa Mkubwa sana Katika Kutokua na Mipaka katika Kila Aina ya Sifa Bora na Bora zaid. Subhanah Allah!

Yaani ukweli hizi njia za Mawasiliano ya Lugha za Viumbe hua kamwe haziwezi kufafanua Maana ya Maneno yenye Sifa zenye Kumzungumzia Muumba yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Kwani kama alivyosema Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: '**Ibn Adam atasema na kufafanua kuhusiana na Maana ya Sifa Tukufu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* hadi Atamaliza, lakini kamwe hatoweza Kufafanua Maana halisi ya sifa hizo Tukufu, kwani yeye Atafafanua Kulingana na Ufahamu wake tu, aliojaaliwa na Mola wake ambao hata hivyo hua hauwezi Kujua Maana halisi ya Sifa za Majina Tukufu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Naam..nimesema hivyo kwa sababu tuko katika kufahamishana maana ya neno *Al Aala* ambalo wengi hua tunalitumia katika kusema *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Na kuna wanaolitumia katika kusema *As Salaam Alaykum wa Rahmat Allahi Taala Wa Barakatuh* n.kNa kuna Umuhimu sana wa Kujua maana ya maneno tunahoyatumia katika Mazungumzo yetu,Dhikr Allah, Maamkizi yetu, Ibada zetu n.k.

Ambapo neno *Al Aala* ni Miongoni mwa maneno tunayoyatumia katika Sujud za nje na ndani ya Ibada ya Sala hususan katika wakati wa Kusujudu.Kwani neno hili ndio neno Kuu la Dhikr ya Sujud.

Kwani ili kufahamu zaidi kuhusiana na neno *Al Aala* basi wacha tuiangalie Aya ya mwanzo ya 87 ya Qur'an ambayo ndio pia iliyobeba Jina linalotokana na Neno Aala ambayo ni *Surat Al Aala*.Na tunapoiangalia Sura hii baso tunaona kua ni miongoni maa Sura ambazo zimeshushwa Mwanzoni mwa kipindi cha Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa salam.*

Na hili kinathibitishwa na ile aya yake ya 6 isemayo:

﴿سَنُقْرِئُكَ فَلَا تَنسَىٰٓ﴾

Sanuqriuka Fala Tansa*(Surat Al Aala 87:6)*

*Tafsir:***NaTutakufanya wewe uwe ni Mwenye Kuisoma(Qur,an ewe *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam*) Na Wala hutoisahau**.

Ambapo maneno ya aya hii yanathibitisha kua huu ulikua ni wakati ambao *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikiwa anapokea Wahyi wa Qur'an huku akiwa hajazoea vizuri bado na hivyo anakhofu kua huenda ataisahau.

Hivyo aya inamthibitishia kua Usiwe na Khofu sisi tutakushuhia na utaisoma na hutoisahau.Yaani Ukiangalia maana ya Maneno ya Aya hii tu, na Kutafakkar basi hua inakutosheleza kufaham japo kidogo maana ya neno *Al aAla* na *Ta'aAla* kulingana na ufahamu wetu wa Kiibn Adam.

Kwani ukiangalia zaid *Surat Al Aala* basi unaona kua Imebeba zaidi Ujumbe wa Tawhid yaani Ujumbe wa Kumpwekesha *Allah Subahanah wa Ta'ala*, na kisha ikabeba Ujumbe wa Maamrisho ya mwenye *Sifa ya Al aAala* na Ukumbusho wa Akhera aliyoiandaa *Al aAla*.Hivyo Jina la Sura hii linaendana sana na Mada zilizomo ndani ya Aya zake.

Na tunapoiangalia aya yake ya mwanzo Sura h hii basi tunaona inasema baada ya *Bismi Allahi Rahmani Rahiim* kua:

﴿سَبِّحِ ٱسْمَ رَبِّكَ ٱلْأَعْلَى﴾

Sabbihi-isma Rabbika Al A'ala*(Surat Al Aala 87:1)*

Tafsir: ***Litukuze Jina la Mola wako Aliekua Juu kabisa Kiutukufu kupita Sifa zote zilizo bora kabisa.***

Hivyo maana ya maneno ya Aya hii ni kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kila anaemuamini na kumfuata kutokana na kujua kua *yeye Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie Muumba kua:'**Litukuze Jina la Mola wako na litangazie kwa Daraja ya Juu zaid ya Utukufu na hivyo Jina la Mola wako lisitumike katika Kuainisha kitu chochote kilicho mbali nae na wala lisitumike kwa kitu chengine chochote isipokua kwa Muumba Mwenyewe.Na kutokana na Aya hii basi tunaona kua Utukufu wa Majina ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* haitakiwi Kutamkwa au kuandikwa kwenye Sehemu isiyokua Nadhifu au isiyokua Tohara.'**

Nakutokana na Aya kua ni yenye kua na Amrisho hilo la Kutukuza Majina Matukufu *ya Allah Subhanah wa Ta'ala.* '**Basi Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua na na Tabia ya kusema *Subhanah Rabbiy Al Aala,* kila walipokua wakiisoma Sura hii baada ya kumaliza Aya yake hii ya Kwanza. Hivyo nasi mimi nawe hua linatakiwa kua ni mwenye kusema hivyo pia.**

Ambapo miongoni mwa waliokua wakifanya hivyo basi alikuwemo *Amir Ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibm *Umar Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu n.k.(Imam Abu Daud)***

Kwani anasema Mujtahid Al *Mutlaq* Imam Ibn Al Mundhiri Al Shafii kua: '*Wakati Allah Subhanah wa Ta'ala* alipoishusha Aya hii ya Mwanzoni ya *Surat Al Aala* isemayo:

﴿سَبِّحِ ٱسْمَ رَبِّكَ ٱلْأَعْلَى﴾

Sabbihi-isma Rabbika Al A'ala*(Surat Al Aala 87:1)*

Tafsir: ***Litukuze Jina la Mola wako Aliekua Juu kabisa Kiutukufu kupita Sifa zote zilizo bora kabisa.***

Basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: '**Fanyeni Hili (la Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'aala)* katika Sujud *zenu'*** *(Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Ibn Majah)*

Ambapo maneno haya pia amesema Ibn Marduwayh, Jarrah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakhshari na Imam Ibn Kathir pia.

Na hii ni kulingana na Hadith ya Uqbah Ibn Amr *Radhi Allah Anhu* isemyo:

عن عُقبةَ بنِ عامرٍ رضيَ اللهُ عنه، قال: ((لَمَّا نزلَتْ: فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ، قال رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم: اجعَلوها في رُكوعِكم، فلمَّا نزلَتْ: سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى، قال: اجعَلوها في سجودِكم))

Amesema Uqba Ibn Amr *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Iliposhushwa *Fasabih BihamdI Rabbika Al Adhiim,* basi alisema *Rasul Allah Salallahuu Aalayhi wa Salam* kua: 'Ijaalieni hii kua katika Rukuu zenu, na iliposhuka *Sabihisima Rabbika Al Aala basi Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alisema kua: 'Ijaalieni hii katika Sujudu zenu'''

Ambapo kwa Upande wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,*Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu* na Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* pia nao walikua kila wakiisoma *Surat Al Aala* katika Sala zao basi mara baada ya Kuisoma aya hii ya Kwanza walikua wakisema: '***Subhana Rabbiy Al Aala.'***

Na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alikua akifanya hivyo pia ambapo siku moja akaulizwa: '**Hivi Jee Ewe Ali unaongeza Maneno ndani ya Qur'an?'**

Ambapo nae akasema: **'La hakika huku si kuongeza kwani sisi tumeamrishwa (na Aya hii) kufanya kitu hivyo nami nimekifanya kitu hicho.'**

Ama kuhusiana na Dhikr za Sujud basi kuna Hadithi isemayo kua;

أَخْبَرَنَا إِسْحَاقُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، قَالَ أَنْبَأَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، عَنِ الأَعْمَشِ، عَنْ سَعْدِ بْنِ عُبَيْدَةَ، عَنِ الْمُسْتَوْرِدِ بْنِ الأَحْنَفِ، عَنْ صِلَةَ بْنِ زُفَرَ، عَنْ حُذَيْفَةَ، قَالَ صَلَّيْتُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَرَكَعَ فَقَالَ فِي رُكُوعِهِ " سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمِ " . وَفِي سُجُودِهِ " سُبْحَانَ رَبِّيَ الأَعْلَى "

Yaaniamesema: **'Is-haq Ibn Ibrahim kua ametumbia sisi Abu Muawwiyah kua amesema Al Amash kua amesema Said Ibn Ubaydah kua amesema Al Mustawrid Ibn Al Ahnaf kua amesema Silat Ibn Zufar kua amesema Hudhayfah Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* kua:'Mimi nilisali pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambapo alipokua akirukuu basi alisema *Subhanah Rabbi Al Adhiim* na alipokua akisujudu basi alikua akisema *Subhanah Rabbi Al A'aala'***(Sunan An Nasai)*

Hivyo hii ni hadith ambayo inatuonesha kuhusiana na Adhkar za Sujud kama vile ilivyokua ikituonesha kuhusiana na Adhkar za Rukuu. Ambapo kama tunavyoona basi inatuonesha kua katika wakati alipokua akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha akawa ni mwenye kuingia katika hatua ya Kusujudu na Kusujudu basi ndani yake Sijda yake hio alikua akisema *Subhanah Rabbiy Al Aaala.*

Na Alhamd lillah tumefahamishana kuhusiana na maana ya neno *Al Aaala,* ambalo tumekua tukilifafanua kwa sababu Mtizamo ya Wanazuoni imeelemea zaidi kwenye aina hii ya Dhikr kuliko katika aina nyenginezo Dhikr nyenginezo kama tutakavyoona hapo baadae. Mbali ya kua Ukweli ni kua Kama ilivyokua kuna Hadith kadhaa zenye kuelezea kuhusiana na Adhkar tofauti za Rukuu basi ndio pia vile vile hli ilivyokua katika upande wa wingi wa Hadith wa Adhakar tofauti za Sujud.

Kwani kuna hadith isemayo kua:

وعنها رضي الله عنها قالت: كان صلى الله عليه وسلم يقول في ركوعه وسجوده: "سبُّوح قدُّوس، ربُّ الملائكة والروح".

Anasema *Ummu ul Muuminina* Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua kila akirukuu na akisujudu basi alikua akisema: *Subuhun Qudusun Rabbi Al Malaikati wa Al Ruhu* - Ametakasika Mwenye Utakatifu Mola wangu, Mola wa Malaika na Ruhi'***(Sahih Muslim)*

Ambapo tunapoiangalia Hadith hii basi tunaona kua inaainisha yale yanayotakiwa kutamkwa ndani ya Ibada katika Kitendo cha Kusujudu, ambayo si maneno mengine yeyote isipokua Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Sifa zake Tukufu.

Kwani Ndani yake Dhikr hii basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiainisha na Kuupandisha Juu zaidi Utukufu wa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* la Al Qudus.

Kwa kusema kua Utukufu ni wako ewe Mwenye Utakatifu zaidi kuliko chochote, Wewe ni uliembali sana na mapungufu ya kua na uchafu na kila kasoro, Wewe ndie Mola wangu, Ndie Mola wa Malaika wote tusiowaona waliotuzunguka Ardhini na walio Mbinguni, Wewe Ndie Mola wa *Ruhi* yaani wa Malaika Jibril.

Kwani maneno haya ya Dhikr ya Hadith hii pia yanafaa kutumiwa kwenye Sijda.

الثالث: عن عائشة رضي الله عنها قالت: ما صلى رسول الله صلى الله عليه وسلم صلاة بعد أن نزلت عليه { إذا جاء نصر الله والفتح} إلا يقول فيها: " سبحانك ربنا وبحمدك، اللهم اغفر لي" ((متفق عليه)).

Kwani anasema *Umm Ul Muuminina Aisha Radhi Allahu Anha* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*alikua mara wa mara katika Rukuu na Sujud akisema: *Subhanak Allahuma Rabbana Wa Bihamdika Allahuma Ighfir li*. Yaani Utukufu Kamilifu ni wako ya Allah, Ewe Mola wetu Na Shukrani zote ni za kustahiki Juu yako. Ya Allah nisamehe Dhambi zangu.'***(Sahih Bukhari na Muslim, Riyadh Salihin, Mishkat Masabih)*

Na kuna Hadith katika Sahih Muslim isemayo kua:

وَحَدَّثَنِي حَسَنُ بْنُ عَلِيٍّ الْحُلْوَانِيُّ، وَمُحَمَّدُ بْنُ رَافِعٍ، قَالاَ حَدَّثَنَا عَبْدُ الرَّزَّاقِ، أَخْبَرَنَا ابْنُ جُرَيْجٍ، قَالَ قُلْتُ لِعَطَاءٍ كَيْفَ تَقُولُ أَنْتَ فِي الرُّكُوعِ قَالَ أَمَّا سُبْحَانَكَ وَبِحَمْدِكَ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ فَأَخْبَرَنِي ابْنُ أَبِي مُلَيْكَةَ عَنْ عَائِشَةَ قَالَتِ افْتَقَدْتُ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم ذَاتَ لَيْلَةٍ فَظَنَنْتُ أَنَّهُ ذَهَبَ إِلَى بَعْضِ نِسَائِهِ فَتَحَسَّسْتُ ثُمَّ رَجَعْتُ فَإِذَا هُوَ رَاكِعٌ أَوْ سَاجِدٌ يَقُولُ " سُبْحَانَكَ وَبِحَمْدِكَ لاَ إِلَهَ إِلاَّ أَنْتَ " . فَقُلْتُ بِأَبِي أَنْتَ وَأُمِّي إِنِّي لَفِي شَأْنٍ وَإِنَّكَ لَفِي آخَرَ .

Amesema Hasan Ibn Ali Al Khulwani na Muhammmad Ibn Rafii, kua ametuhadithia Abd Razzaq kua ametuambia Ibn Jurayj kuaalimwambia Ataa : 'Hivi imekuaje hadi ukwa unasema uyasemayo katika Rukuu?' Ambapo Ataa akasema: 'Ama kuhusiana na *Subhanaka wa Bihamdika La ilaha Illa* Anta basi ameniambia mimi Ibn Mulaykah kua: 'Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: Mimi niligundua kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hayuko pamoja nami Kitandani. Nami nikadhania kua labda ameenda kwa Mmoja kati ya Wake zake wengine. Hivyo nikaanza kumtafuta na kurudi huku nikimuona akiwa katika hali ya Kurukuu au Kusujudu akiwa anasema:*Subhanak Wa Bihamdika La Ilaha Illa Anta* - Utukufu kamilifu na Shukurani stahiki ni zako, Hakuna Mungu isipokua wewe Peke yako.

Aisha *Radhi Allahu Anha* anaendelea kusema kua: "**Mimi nikasema Baba yangu na Mama yangu watolewe Muhanga, kwani mimi nilikua Nafikiria kuhusiana na Jambo Jengine wakati wewe *(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam)*Ukiwa Unajishughulisha na Jambo Jengine** *(Sahih Muslim)*

Ambapo kuna hadithi nyengine kama hii ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambayo anasema alipomtafuta basi mikono yake ikagusa miguu ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alikua katika Hali ya Sujud huku akiwa ni mwenye kusema:

"اللهم إني أعوذ برضاك من سخطك، وبمعافاتك من عقوبتك، وأعوذ بك منك، لا أحصي ثناء عليك أنت كما أثنيت على نفسك"

Allahuma inni Audhu Biridhaka Min Sakhtika, Wa bi Muafatika Min Uqubatika.Wa Audhu bika minka la Uhsi Thanaan Ilayka, Anta kama Athnaita aAla Nafsika - Yaani Najikinga Kutokana na Radhi zako dhidi ya Hasira zako, na Nakijikinga kutokana na Usamehevu wako Dhidi ya Adhabu zako na mimi ni mwenye kutoka Kwako na kwako ndio Marudio yangu Nakusifu na Nakutukuza na siwezi Kukutukuza kama Ipasavyo.'*(Imam Muslim, Imam Ibn Khuzaymah, Imam Ibn Al Mundhir Imam Ibn Hibban, Imam Al Hakim, Imam Al Bayhaqi, Ibn Abd Al Barr na Imam At Tahawi, Riyadh Salihina)***

Naam hizo ni baadhi tu ya mifano ya Dhikr na Dua ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alizokua akizisoma katika Sala zake. Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kuhisiana na Dhikr za Ndani ya Rukuu na Sujud kua: **'Na fahamuni kua Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kurukuu na Kusjudu hua ni Sunna na si Wajib'***(Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo huo ni mmoja kati ya Mitizamo miwili juu ya Suala hili la Tasbih na Dhikr ndani ya Rukuu na Sujud.Na Mtizamo wa Pili hua ni ule usemao kua Kutamka Dhikr na Tasbih katika Kusjudu na Kurukuu hua ni Wajib.

Kwani Mtizamo wa Kwanza kuhusiana na kua Dhikr Allah ndani ya Sujud hua ni Sunna basi ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii,Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhhab ya Imam Malik na pia kua Mtizamo mmoja kutoka kwa Miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahamd Ibn Hanbal.

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriya Yajya Ibn Sharaf An Nawawi anafafanua zaidi kwa kusema kua: '**Ama kuhusiana na Dhikr Allah na Tasbih Katikka Rukuu na Sujud, na Kusema *Sami Allahu liman Hamida, na Rabbana wa Laka Al Hamd na Takbir al* Intiqam (isiyokua ya Ihram)**. **Basi yote haya ni Sunna na Si Wajib hivyo kama Mtu akiwacha basi hua Hafanyi Dhambi na Sala yake hubakia kua ni Sahih iwe imeachwa kwa Makusudi ama kwa kusahau. Lakini hua ni bora Kufanya kuliko kuacha kwa Makusudi.**

Hivi Ndivyo Isemavyo katika Skuli ya Madhhab yetu, na Ndivyo alivyosema Imam Malik na Imam Abu Hanifa, na Wanazuoni wengi wengineoShaykh Abu Hamid(Imam Ahmad Ibn Abu Tahir Muhammad Ibn Ahmad Al Isfaryini Al Shafii) amesema kua: 'Mtizamo huu ni Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni.'

Na Mwandishi wa Al Hawi(Al Qadhi, Al Faqih Imam Ali Ibn Muhammad Al Mawardi) amesema kua: 'Haya ndio Mafundisho ya Mtizamo wa Wanafiqh Wote.'

Imam Is-haq Ibn Rahawayh Al Shafii yeye amesema kua: 'Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Rukuu na Sujud hua ni Wajib na hivyo kama Mtu akiwacha kwa Makusudi basi Sala yake hua ni Batili na kama akiwacha kwa kusahau basi Sala hua haibatiliki. Imam Abu Daud nae amesema kua Imam Al Khattabi ameonesha Chaguo lake kua Kufanya Dhikr Allah na Tasbih katika Rukuu na Sujud hua ni Wajib.

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: Ama kuhusiana na Dhikr Allah na Tasbih Katikka Rukuu na Sujud, na Kusema Sami Allahu liman Hamida, na *Rabbana wa Laka Al Hamd* na *Takbir al Intiqam* (isiyokua ya Ihram) vyote hivi ni Wajib hivyo kama Mtu akiwacha baadhi yake kwa kukusudia basi Sala yake hua ni Batili na akiwa amesahau basi Sala haibatiliki,ila itambidi alete Sijdat SahwNa pia Imam Ahmad amenukuliwa akisema kua ni Suna'*(Al Majmuu)***

Kwani kama tunavyoona kua Mtizamo wa pili ambao usemao kua Kufanya Dhikr Allah na Tasbih katika Rukuu na Sujud kua ni Wajib, ni Mtizamo wa Imam Is-haq Ibn Rahawayh ambae ni rafiki yake Imam Ahmad Ibn Hanbal na wote kwa pamoja walikua ni Wanafunzi wa Imam Muhammad Idris Al Shafii katika wakati alipokua akiishi Mjini Baghdad.

Na bila ya shaka ingawa Maimam wote watatu hawa wana Darja kubwa sana ya Ilm, lakini hata hivyo. Imam Ahmad Ibn Hanbal alianzisha Madhhab yake lakini kwa Upande wa Imam Is-haq Ibn Rahawayh basi yeye alibakia kwenye Madhhab ya Imam Al Shafii.

Na ndio maana basi hua tunaona kua kuna baadhi Imam Ahmad Ibn Hanbal anaetumia Mitizamo ya Imam Ibm Rahawayh, na baadhi anatumia ya Imam Al Shafii na baadhi Mitizamo yake mwenyewe n.k. na kuna kesi ambazo Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua kwanza akitumia Mitizamo ya Imam Al Shafii lakini baadae akaamua kufuata.

Mitizamo ya Imam Ibn Rahawayh baada ya kuipata, mbali ya kua Imam Ibn Rahawayh mwenyewe alikua akiwacha baadhi ya Mitizamo yake ambayo Imam Ahmad anaitumia baada ya Imam Ibn Rahawayh mwenyewe kuipata Mitizamo ya Imam Al Shafii.Na hii inatuthibitishia Umuhimu wa watu kua ni wenye Kufuata Maimam wa Madhhab kwani Maimam ndio wenye kujua zaidi kuhusiana na Ilm ya Dini.Ila wenye kufahamu Umuhimu huu hua ni wenye Kujua tu, kwani wasiojua hukuWakijiona kua ni wenye kujua hua ni wenye Mitizamo ya kutofuata Maimam, Jambo ambalo sio Sahih na ni upotovu.

Kwani Kama ikiwa Imam Is-haq Ibn Rahawayh ambae alikua na Ilm Kubwa kuliko Imam Ahmad Ib Hanbal, kiasi ya kua Imam Ahmad Ibn Hanbal mwenyewe alikua anaifuata Mitizamo yake Ibn RahawayhLakini mbali ya kua na Ilm yote hio,lakini bado alikua ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, yaani anamfuata Imam Al Shafii.

Na tukimwangalia Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhamamad Al Ghazali ambae nae alikua na uwezo hata wa Kuanzisha Madhhab yake kutokana na Ukubwa wa Ilm yake. Kwani kitabu chake cha Ihya Ulum Ad Din tu kinashika sehemu ya 3 baada ya Qur'an na Sunna katika Uislam. Lakini hata hivyo nae aliamua Kumfuata Imam Al Shafii katika Madhhab yake. Na ukweli ni kua kuna Mifano Mingi sana inayotuonesha Umuhimu wa kufuata Maimam wa Madhhab kwa Wanaotafakkar!

Naam, Miongoni mwa Wanafunzi wakubwa sana Kiilm wa Imam Mkubwa sana Kiilm ambae ni Imam Al Muhaqqiqin Al Faqih Imam Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii alikuwepo yule anaejulikana kama Imam Zayn Ad Din Ibn Abd Al Aziz Al Malibari Al Shafii

Kwani anasema Imam Zayn Ad Din Al Malibari kuhusiania na Tasbih na Dhikr katika Rukuu na Sujud kua: **'Ni Sunna kwa Mtu anaesali *kusema Subhanah Rabbiy Al Adhiim wa Bihamdihi* mara tatu katika Wakati wa Kurukuu, na ni Sunna kusema *Subhanah Rabbiy al Aala Wabihamdihi* mara tatu katika wakati wa Kusujudu'***(*Fathul Mu'in)*

Ambapo kwa upande mwengine wa wale wanaosema kua Tasbih na Dhikr hua ni Wajib katika Rukuu na Sujud basi tunaporudi kwa Upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na kumuangalia Imam Muwafaqa Ad Din Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi tunaona kua yeye anasema kua: '**Kinachojulikana kwa Madhhab ya Imam Ahmad ni kua;Takbir Al Itiqaam za kuenda chini na kuinuka, Tasbih katika Wakati wa Kurukuu na Kusujudu, Sami Allahu Liman Hamida, Rabbana wa Laka Al Hamd na Rabbi Ighfirlii wa Arhamni baina ya Sijda mbili na Tashahhud ya Kwanza, basi Vyote hivi hua ni Wajib.**

Lakini hata hivyo pia katika Madhhab ya Imam Ahmad pia kuna Mtizamo pia usemao kua vitu hivyo ni Sunnah na wala Si Wajib, ambao huu ndio Mtizamo wa Wanafiqh wengi Sana.'*(Al Mughni)*

Kwani tukirudi kwa upande wa Khatima Al Muhaqqiqin wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambae ni Imam Muhammad Amin Ibn Amr Ibn Abd Al Aziz Ibn Aabidin Al Shaami Al Hanafi basi yeye anasema kua: '**Ni Sunna Iliyothibitishwa katika Rukuu kusema *Subhanah Rabbiy Al Aadhiim* mara tatu na kusema *Subhanah Rabbi Al aAala* katika Kusujudu Mara tatu, na kuacha Sunna iliyothibitishwa hua Hakupendekezwi.Na hivyo Ni Wajibu Kufanya Tasbih hizo mara 3'***(Maraqi Al Falah)***

Natukirudi kwa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi basi tunaona Kia pia amesema kua: '**As-hab wa Madhhab yetu wamesema kua ni Sunna kusema *Subhanah Rabbiy Al Aadhiim wa Bihamdihi* katika Rukuu na kusema *Subhanah Rabbiy Al Aaala Wabihamdihi* katika Sujud**. **Na Miongoji mwa Wanazuoni waliotoa Uthibitisho wa Maandiko wa Kusema neno Wabihamidhi ni pamoja na Al Qadhi Abu Tayyib Al Isfarini, Qadhi Husein, Mwandishi wa Kitabu cha Shamail, Hujjat Ul Islami Imam Al Ghazali na wengineo'***(Al Muhadhdhab)*

Ambapo kama tulivyosema hapo awali kuhusiana na matumizi ya neno *Wabihamdihi* kwa kusema *Subhanah Rabbi Al Adhiim Wabihamdihi na Subhanah Rabbi Al Aala Wabihamdihi* katika Tasbih na Dhikr za Rukuu na Sujud kutoka katika Hadith ya Hudhayfah *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa Imam Ad Daraqutni, na kwa Uqbah Ibn Amir *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa Imam Abu Daud pia katika hadith ya Abd Allah Ibn *Masud Radhi Allahu Anhu* isemayo kua:

كان رسول الله صلى الله عليه وسلم إذا ركع قال : سبحان ربي العظيم وبحمده ثلاثا . وإذا سجد قال : سبحان ربي الأعلى وبحمده ثلاثاف.

'Alikua *Rasul AllahSalallahuAlayhi wa Salam* akirukuu basi ni mwenye kusema*Subhanah Rabbi Al Aadhiim Wa Bihamdih*mara tatu na anaposujudu husema*Subhanah Rabbi Al Aalaa Wa Bihamdihi mara tatu*'*(Sunan Abu Daud)***

Na tunapomuangalia Imam Ad Daraqutni pia basi tunaona kua Abd Allah Ibn *Masud Radhi Allahu Anhu* nae pia amesema kua: '**Imejumuishwa katika Sunnah kwa Mtu *kusema Subhanah Rabbi Al Aadhiim Wa Bihamdihi* katika Rukuu na na kusema *Subhanah Rabbi Al Aala Wabihamdihi* katika Sujudu***(Imam Ad Daraqutni)***

Na Ingawa Baadhi ya Wanazuoni wanasema kua kuna Udhaifu wa Minyororo ya Watu walionukuu Hadith hizi, lakini hata kisharia basi Hadith yenye kasoro hua inaweza kutumika. Pale inapokua Hadith husika zinapeana nguvu wenyewe kwa wenyewe kwa Wingi wake, au kwa kupewa nguvu na hadith nyengine Sahih, au kwa kuipa nguvu hadith nyengine.Ambapo Katika hadith hizi zenye kuelezea Sunnah hii ya kuongezea neno Wabihamdihi ni hadith zenye Sifa ya Hasan Li Ghairihi.Yaani Hadith ambazo Waliozinukuu hua Wanafanya Makosa lakini hata hivyo hua hawesemi Uongo.

Kama anavyosema Al Hafidh Al Faqih Imam Muhammad Ibn Alan Al Sadiqi Al Shafii kua: '**Hadithi ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi AllahuAnhu* inatuonesha kua yeye Ibn Masud Radhi Allahu Anhu aliporukuu alisema: *Subhanah Rabbi Al Adhiim wa Bihamdihi* na aliposujudu Alisema *Subhanah Rabbi Al aAla Wabihamdihi,* na kisha akasema kua Hivi ndivyo alivyokua akisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Imam Ibn Alan anaendelea kusema kua: **'Hadith hii ni Dhaifu, na Sanad yake imekatika, lakini hata hivyo hadith hii inapewa nguvu na kuungwa mkono na Hadith ya Uqbah Ibn Amir *Radhi Allahu Anhu iliyonukuliwa na Imam Abu Daud.'***

Kwani Imam Ibn Alan Al Shafii anaendelea kusema kua: **'Na hata hivyo hua hakuna kosa kwa Mtu kuongeza Dhikr katika Maombi na kufanya hivyo kunahalalishwa na Hadith ya Rifaa Ibn Raafi Al Zaki *Radhi Allahu Anhu* isemayo Siku moja tulisali *na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliponyanyua Kichwa kutoka kwenye Rukuu na kusema *'Sami Allahu Liman Hamida'***

Kisha mtu mmoja akasema Nyuma yake *Rabbana wa Laka Al Hamd Hamdan Taiban Mubarakan fiih*.'

Basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: "'Jee ni nani aliesema vile?'

Yule Mtu akajibu :Ni Mimi hapa *Ya Rasul Allah!*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema;**

Nimewaona mimi Malaika zaidi ya 30 wakipigana kwa ajili ya kila mmoja awe wa mwanzo kuyaandika maneno hayo"*(Imam Ibn Alan Futuhat Rabbaniyah)*

Na amesema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani kua: '**Hadith hii ni yenye kuthibitisha kua inakubalika kusoma Dhikr yeyote inayofaa katika Sala bila ya hata kua na Uthibitisho'**
(Fat-h Al Bari)

Kwani hio ni kwa Upande wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii lakini kwa upande basi kuna wale wanaosema *Subhanah Rabbi Al Adhiim,* tu mara tatu katika Rukuu na kusema *Subhanah Rabbi Al Aala* tu mara tatu katika Kusjudu.

Na hivyo hii haimaanishi kua hawa wanakosea la hawakosei na hii ni kwa sababu ya kama tulivyoona kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wao wanasema kua Inapendekezwa zaid kuongeza neno Wabihamdihi.

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Daud ambae ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii pia basi amesema kuhusiana na kuongezwa kwa Neno *Wa Bihamdihi* kua: '**Ama kuhusiana na Wabihamdihi basi hakika tunaogopa kua huenda Ikasahauliwa kutokana na Kutohifadhiwa na kutotumiwa.'**

Ambapo kwa Upande wa Mujtahid Al Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri basi yeye anasema kua: **'Aliulizwa Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na Nyongeza hii ya Wabihamdihi katika Tasbih za Rukuu na Sujud ambapo nae akasema:'Ama mimi sisemi maneno hayo Wabihamdihi na ushahidi wangu ni Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua mara kwa mara akisema katika *Rukuu Subhanaka Allahuma Rabbana Wabihamdika* na akisema kwenye Sujud *Subhanaka Allahuma Rabbana wa Bihamdika.***

Na hivyo kama Mtu atakua anaongeza kwa kusema Wabihamdihi basi hua hamna Tatizo,na hii ni kwa sababu yamesemwa hayo kwenye Hadith ya Hudhayfa *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema hivyo katika Rukuu zake na Sujud zake.'

Ambapo kwa Upande wa Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali anasema pia kua: **'Nyongeza hii pia imetajwa kutoka kwa Imam Abd Rahman Ibn Abi Layla. Kwa hivyo inawezekana Ikawa Imam Ahmad Ibn Hanbal hakuitumia kutokana na kuona kua isiyotosheleza vigezo vyake.'**

Kwa maana hio basi Kuongezea neno *Wabihamdihi* katika Tasbih za Rukuu na Sujud hua ni Sunna ambayo imethibitika kwenye Hadith.Na hivyo ni Vizuri kuitumia kwani inakupandishia Darja zaid ya Sala yako, na pia Mtu asipoitumia basi hua hamna tatizo. Hivyo Tasbih za Sala za Rukuu na Sujud hua ni Sunna na zinakupandishia Darja Sala yako, na hivyo haitakiwi kuzipuuza, kwani Ibn Adam hua tunahitaji kujaribu Kuchuma Malipo bora zaidi ndani ya Ibada zetu, hususan Ibada ya Sala.

Na hivyo Kupuuza basi hua ni kuonesha Dharau ndani ya Sala,na ndio maana akasema Imam An Nawawi kua: '**Mtu anaepuuza mara kwa mara Tasbih za Kurukuu na Kusjudu ndani ya Sala hua ni Mwenye Kughafilika na Ibada zake zinazojumuisha Imani ya Dini yake**. **Na anaeghafilika na Dini yake basi hua ni Mwenye Kukataliwa Ushahidi wake.'***(Al Majmuu)*

Kwani tumeona kulingana na Vithibitisho kua kufanya Tasbih kwa Kusema *Subhanah Rabbi Al Adhiimwa Bihamdihi* katika Rukuu, na kusema *Subhanah Rabbi Al aAla Wabihamdihi* katika Sujud kua ni Sunna.

Na hii ni kulingana na Maneno na Vitendo vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala zake, kua alifanya Tasbih kwa mpangilio huo wa kutofautisha baina baina ya Tasbih za Rukuu na za Sujud.
Ambapo anasema Imam An Nawawi kua: '**Kama Mtu atakua ni mwenye Kusahau, au atakua ni mwenye kuiacha basi Sala yake hua haitobatilika na wala haitohitajika kwa mtu huyo Kuleta Sijdat Sahw'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Lakini sasa kwa upande mwengine huenda watu wakajiuliza suali lifuatalo: '**Kama ikiwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam ameamrisha Tasbihi hizi kulingana na Sehemu husika,hivyo jee kwa mfano imetokea kua Mtu ameingia Katika Rukuu na kisha akasema Subhanah Rabbi Al aAla Wabihamdihi, ambayo ni Dhikr ya Sujud**. **Au Labda Imetokea katika Sujud mtu akasema Subhanah Rabbi Al Adhiim wa Bihamdihi badala ya kusema *Subhanah Rabbi Al Aala Wabihamdihi*. Jee Hukmu yake itakuaje kuhusiana na hili?'**

Naam..Anasema Imam Sulayman Al Jamal Al Shafii katika *Khashiah Al Jamal* kua: '**Kama ikitokezea kua Mtu anaesali amerudia katika sehemu sio yake Maneno ambayo yenye Darja ya kua ni Nguzo ya Sala, basi Mtu huyo itambidi kufanya Sijdat Sahw**. **Lakini Kama ikiwa Mtu ametamka Tasbih ya Sunna katika sehemu sio yake, basi hua haina haja ya Mtu huyo kufanya Sijdat Sahw'** *(Hashiyyah Al Jamal)*

Kwani anasema Mwanafiqh Imam Sulayman wa pili wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambae ni Imam Sulayman Ibn Muhammad Al Bujairimi Al Shafii kua: '**Kama ikitokea kua Mtu atasoma Kisomo ambacho ni Sunnah katika sehemu sio ndani ya Sala yake, basi hua haina haja kwake kufanya Sijdat Sahw, isipokua pale itakapotokea Tatizo la kua Amesoma Sura nyengine zaidi ya Al Fatiha nje ya Hatua ya Kisimamo cha Sala**.*'(Hashiyyah Al Bujairimi)*

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam An Nawawi wa pili wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambae ni Abd Al Muith Ibn Muhammad An Nawawi Al Jawi Al Shafii katika kitabu chake cha Nihayat Al Zain Fi Al Irshad Al Mubtadin - Fiqh Madhhab Al Shafii.

Kwa maana hio basi kutokana na kua Tasbih za Rukuu na Sujud ni Sunnah basi hata kama ikitokea kua

Mtu amejichanganya na hivyo ya Rukuu kaweka kwenye Sujud na ya kwenye Sujud kaweka kwenye Rukuu, au labda ametamka Tasbih Moja katika Sehemu zote mbili yaani iwe ya Rukuu kaitamka na kwenye Sujud pia au ya Kwenye Sujud kaitamka na kwenye Rukuu hio hio, basi hii hua hamna tatizo. Yaani Sala yake haijabatilika na wala haitompelekea yeye pia Kufanya Sijdat Sahaw.

QUR'AN KATIKA SUJUD

❖❖❖

Hivyo Kulingana na Vithibitisho vya Hadith na Mitizamo ya Wanazuoni basi tumeona kua kufanya Adhkar na Tasbih ndani ya Sala katika Hatua za Rukuu na Sijda hua ni Sunna ambayo kutofanywa kwake hua haipendekezwi.Na bila ya Shaka hua pia hamna tatizo lolote kama ikitokea kua Mtu amejichanganya katika Usomaji wa Tasbih hizo kwa kuitamka Tasbih ya kwenye Rukuu wakati ukiwa kwenye Sijda n.k

Ingawa hii hua haitokei kwa wale wenye Kuhudhurisha Nyoyo zao ndani ya Sala na hivyo kua na Khushuu lakini kwa baadhi ya watu hua inawatokezea kwa baadhi ya wakati pia na ndio maana ikabidi tuiangalia na kufahamishana juu yake.

Kwani kwa upande mwengine basi inabidi tufahamishane pia kuhusiana na kutoruhusika Kufanya Kisomo cha Qur'an ndani ya Rukuu na Sijda pia kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na jambo hili katika Hadith iliyonukuliwa na Abd Allah Ibn *Abbas Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema:

حديث عبد الله بن عباس رضي الله عنهما قال: كشف رسول الله صلى الله عليه وآله وسلم الستارة والناس صفوف خلف أبي بكر رضي الله عنه، فقال: «أَيُّهَا النَّاسُ، إِنَّهُ لَمْ يَبْقَ مِنْ مُبَشِّرَاتِ النُّبُوَّةِ إِلَّا الرُّؤْيَا الصَّالِحَةُ؛ يَرَاهَا الْمُسْلِمُ، أَوْ تُرَى لَهُ، أَلَا وَإِنِّي نُهِيتُ أَنْ أَقْرَأَ الْقُرْآنَ رَاكِعًا أَوْ سَاجِدًا، فَأَمَّا الرُّكُوعُ فَعَظِّمُوا فِيهِ الرَّبَّ عَزَّ وَجَلَّ، وَأَمَّا السُّجُودُ فَاجْتَهِدُوا فِي الدُّعَاءِ، فَقَمِنٌ أَنْ يُسْتَجَابَ لَكُمْ

Amesema Abd Allah Ibn *Abbas Radhi Allahu Anhu*kua : '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliteremsha Pazia lake katika Wakati a Ugonjwa wake, katika wakati ambao Watu walikua wakisalishwa na Abu Bakar *Radhi Allahu Anhu*. Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Enyi Watu, hakuna kilichobakia katika Ubashirio wa Unabii isipokua Ndoto Njema anazoomneshwa Muislam. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema :Hakika mimi nimekatazwa kusoma Qur'an katika Wakati ambao nikiwa kwenye Rukuu na Sujud,hivyo Mtukuzeni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani ya Rukuu na Sujud Zenu, na zidisheni Kuomba Dua ndani ya Sijda kwani Mtajibiwa' *(Sahih Muslim)*

Na akasema *Amir ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua:

وما أخرجه أيضًا من حديث علي بن أبي طالب كرم الله وجهه قال: "نَهَانِي رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وآله وَسَلَّمَ عَنْ قِرَاءَةِ الْقُرْآنِ وَأَنَا رَاكِعٌ أَوْ سَاجِدٌ

‘***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **amenikataza mimi Kusoma Qur'an katika Wakati wa Kurukuu na Kusujudu.’** *(Sahih Muslim)*

Kwani Hadith mbili hizi zinatuonesha kua Maneno haya aliyasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Kipindi cha Mwishoni mwa Uhai wake.Ambapo ndani yake Maneno haya basi alikua akibashiria kua hakutokua na Wahyi wowote utakaoshuka baada yake na hivyo hakutokua na Unabii mwengine. Na lakini hata hivyo kuna watu ambao *Allah Subhanah wa Ta'aala* atawajaalia kua ni wenye kuoneshwa Usingizini kuhusiana na mambo tofauti ambayo ni yenye Ukweli ndani yake iwe ukweli wa habari nzuri, au Mbaya au Maonyo n.k

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamalizia kuweka wazi kua imekatazwa kusoma Qur'an katika Rukuu na Sijda za Ndani ya Sala.Na hii ni kwa sababu ndani yake Hatua hizo hua mnatakiwa Kufanywa Tasbih, Dhikr Allah na Kuomba Dua tu.

Na kutokana na Hadith hizi basi Wanazuoni wanakubaliana kua Kusoma Qur'an ndani ya Rukuu na Sujud hua ni Makruh yaani hua ni Kufanya Kitukinachokirihisha. Ambapo anasema Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qaylubi Al Masri Al Shafii kua: ‘**Kusoma Qur'an Ndani ya Sala katika Wakati Usiokua wa Kisimamo na kisha Mtu akakududia Kusoma Qur'an ndani yake basi hua ni Makruh.’**

Na akasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Bahadir Al Zarkashi Al Shafii kua: ‘**Hua ni Makruh Kusoma Qur'an kwa Kusudio la Kusoma Qur'an ndani ya Rukuu na Sujud**. **Lakini kama Ikiwa mtu ataisoma kwa Kusudio la kuomba Dua na Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi huaNi sawa na Kusoma Qunutkwa Kutokana na kusoma aya husika.’**

Ambapo anasema pia Imam Al Mujaqqiqin Shaykh Ul Islami Imam Ahmad Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii katika Tuhfah Al Muhtaj kua: ‘**Kusoma Qunut kwa Kisomo cha Aya ya Qur'an hua inaruhusika katika Sehemu ya Kusoma Dua ndani ya Sala hua inakubalika na wala haikirihishi.’**

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi katika Kitabu chake cha Al Adhkar ambamo ndani ya Imam An Nawawi amesema kua pia: ‘**Wanazuoni Wanakubaliana kua ni Makruh Kusoma Qur'an katika Rukuu na Sujud.’**

Al Allamah Imam Mullah Ali Al Qari Al Hanafi amesema katika Marqaat Al Mufatifah Sharh Mishkat Al Masabih: **‘Rukuu na kusujudu ni hali mbili zinazoashiria unyenyekevu na zinafaa kwa ajili ya dua na utukufu, hivyo basi. Kusoma Qur’an ndani yake kumeharamishwa kwa kuiheshimu Qur’ani Tukufu na kumtukuza msomaji wake, ambaye anasimama katika cheo cha Mjuzi mwenye kujua juu ya kila kitu.’.**

Kwani amesema Al Hafidh, Al Faqih Imam Jamal Ad Din Abd Allah Ibn Yusif Al Zaylai Al Hanafi kua ‘**Kusoma Qur'an katika Wakati usiokua wa Kisimamo hua ni Makruh kama mtu atakua ni mwenye Kuisoma kwa nia ya kua ni Kisomo cha Qur'an.’**

Na akasema Imam Al Saawi Al Maliki kua: ‘**Kusoma Qur'an ndani ya Rukuu na Sujud hua ni Makruh, isipokua pale mtu atakaposoma kwa nia ya Kua ni Dua.’**

Ambapo anasema Imam Taqi Ad Din Abu Muhammad Ibn Ali Ibn Wahab Ibn Mutti Ibn Abi Taa Ibn Daqaiq Al Idd Al Masri Al Shafii kuhusiana na Hadith hizikua: '**Bila ya Shaka Kusoma Dua ndani ya Rukuu inaruhusika.'**

Hivyo Wanazuoni wameeleza hekima ya kukataza kusoma Qur'an huku ukirukuu na kusujudu. Kama walivyotaja kwamba Qur'ani Tukufu ndio ukumbusho mkubwa na muhimu zaidi, na mahali pake ni wakati wa kusimama, sio wakati wa rukuu na kusujudu. Kwa ajili ya kuiheshimu Qur'an na kumtukuza msomaji wake, na kwa sababu rukuu na kusujudu ni hali mbili zinazoashiria kujisalimisha na kunyenyekea, na hivyo dua ndio zinazofaa kwa hilo.

DUA KATIKA SUJUD

❖❖❖

Naam, Hivyo Wanazuoni wanakubaliana kua Haikubaliki Kusoma Qur'an katika Rukuu wala katika Sujud wala katika Sehemu nyengine yeyote ile ndani ya Sala isipokua katika sehemu ya Qiyam, yaani Kisimamo cha Sala.

Ambapo Hata Hivyo basi Wanazuoni wanakubaliana kua Inaruhusika Kwa Mtu kua ni mwenye Kusoma Qur'an katika Rukuu, Katika Kisimamo cha Baada ya Rukuu au SujudKwa Nia au Lengo la kua Aya husika zisomwazo si kwa ajili ya Kisomo cha Qur'an bali ni kwa ajili ya Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo hua ni Aya za Tasbih, au kua ni kwa ajili ya Kuomba Dua kwa kua ni aya zenye Dua ndani yake.

Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Dua katika Sujud zake kama inavyosema Hadith ifuatayo:

وَحَدَّثَنِي أَبُو الطَّاهِرِ، حَدَّثَنَا ابْنُ وَهْبٍ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ سَلْمَانَ الْحَجْرِيِّ، عَنْ عُقَيْلِ بْنِ خَالِدٍ، أَنَّ سَلَمَةَ بْنَ كُهَيْلٍ، حَدَّثَهُ أَنَّ كُرَيْبًا حَدَّثَهُ أَنَّ ابْنَ عَبَّاسٍ بَاتَ لَيْلَةً عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ فَقَامَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم إِلَى الْقِرْبَةِ فَسَكَبَ مِنْهَا فَتَوَضَّأَ وَلَمْ يُكْثِرْ مِنَ الْمَاءِ وَلَمْ يُقَصِّرْ فِي الْوُضُوءِ . وَسَاقَ الْحَدِيثَ وَفِيهِ قَالَ وَدَعَا رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم لَيْلَتَئِذٍ تِسْعَ عَشْرَةَ كَلِمَةً . قَالَ سَلَمَةُ حَدَّثَنِيهَا كُرَيْبٌ فَحَفِظْتُ مِنْهَا ثِنْتَىْ عَشْرَةَ وَنَسِيتُ مَا بَقِيَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " اللَّهُمَّ اجْعَلْ لِي فِي قَلْبِي نُورًا وَفِي لِسَانِي نُورًا وَفِي سَمْعِي نُورًا وَفِي بَصَرِي نُورًا وَمِنْ فَوْقِي نُورًا وَمِنْ تَحْتِي نُورًا وَعَنْ يَمِينِي نُورًا وَعَنْ شِمَالِي نُورًا وَمِنْ بَيْنِ يَدَىَّ نُورًا وَمِنْ خَلْفِي نُورًا وَاجْعَلْ فِي نَفْسِي نُورًا وَأَعْظِمْ لِي نُورًا " .

Amesema Abu Tahira kua amesema Ibn Wahbi kua amesema Abd Rahman Ibn Salmana Al Hajrii kua amesema Uqayl Ibn Khalid kua amesema Salama Ibn Quhayl kua amesema Qurayb kua: Amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: Niliutumia Usiku wangu kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoka Usiku na na kusimama kwenye kibuyu

cha maji na kujimiminia na kutia Udhu ambao hakutumia maji mengi wala kidogo katika Udhu wake, na sehemu ya hadith iliyobakia inasema hivyo hivyo, na katika hii inataja kua katika Usiku wa siku hii *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*aliomba Dua mbele ya Allah Subhanah wa Ta'ala kwa kutumia maneno 19, ambapo Qurayb anasema kua Nakumbuka maneno 12 tu kati ya hayo, na yaliyobakia nimeyasahau, ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema:

Allahuma Ij-aAl fii Qalbi Nuran - Ya Allah Niajalie Katika Moyo wangu Nuru.
Wa Fii Lisani Nuran – Na katika Ulimi wangu Nuru.
Wa Fi Sam-ii Nuran - Na katika Masikio yangu Jaalia Nuru.
Wa fii Basri Nuran - Na Katika Mtizamo wangu Jaalia Nuru.
Wa Aan Al Yamini Nuuran -Na kwa upande wa Kulia Kwangu Nuru.
Wa Aani Shimali Nuran - Na Kushoto kwangu Nuru.
Wa Fawqi Nuran wa Tahtii Nuran - Na Juu Yangu Nuru na Chini yangu Nuru.
Wa Min Bayni Yaddaya Nuran - Na baina ya mikono yangu yangu Nuru.
Wa Min Khalfii Nuran - Na Nyuma yangu Nuru.
Wa Ij-aAli Fii Nafsi Nuuran - Na nijaalie Katika Nafsi yangu Nuru.
Wa Adhim Li Nuran – Na nitukuze kwa Nuru.*(Sahih Muslim)*

Ambapo hii ni hadith inayoonesha Mifano ya Duaa ambazo Mtu unatakiwa kuomba katika wakati unapokua katika Sujud.Na bila ya shaka kama tunavyoona katika Hadith hii ambayo imenukuliwa na Imam Ahmad, Imam Bukhari, Imam Ad Daraqutni kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anaomba Kua ajaaliwe awe kua ni mwenye Nuru katika Kila Hali yake na kila Mazingira yake na yeye mwenyewe Awe Nuru.

Na amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua: Niilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema hukua akiwa amesjudu kua:

وعن عائشة: أنها فقدت النبي صلى الله عليه وسلم من مضجعه، فلمسته بيدها، فوقعت عليه وهو ساجد، وهو يقول: "رب، أعط نفسي تقواها، وزكِّها أنت خير من زكاها، أنت وليها ومولاها".

Rabbi Aatta Nafsi Taqwaaha - Ewe Mola wangu Ipe Nafsi yangu Taqwa.
Wazakiha Anta Khayru man Zakkaha - Na Itakase kwani wewe ni m-bora wa Wenye Kutakasa.
Anta Waliiha wa Mawlaha - Wewe ndie Walii wake na Mola wake Nafsi yangu.

Na pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba katika Sujud Dua ifuatayo:

وكان صلى الله عليه وسلم يقول وهو ساجد: "اللهم اغفر لي خطيئتي وجهلي، وإسرافي في أمري، وما أنت أعلم به مني. اللهم اغفر لي جِدِّي وهزلي، وخطئي وعمدي، وكل ذلك عندي، اللهم اغفر لي ما قدمت وما أخرت، وما أسررت وما أعلنت، وأنت على كل شيء قدير

Allahuma Ighfirli Khatayati Wa Jahlii - Ya Allah Nisamehe Dhambi zangu na Ujinga wangu.
Waisra fii Fiy Amri - Na Israfu katika Mambo yangu.
Wama Anta Aalamu Biha minni - Na yake unayoyajua zaidi yangu.
Allahuma Ighfirli Jiddiyi wa hazliy - Ya Allah Nisamehe Uzito wangu na Mzaha wangu.
Wa Khatayya wa aAmadiy - Na makosa yangu na Nia yangu.
Wa Kul dhalika Aan-dii - Na yote hayo ni yangu.

Allahuma Ighfrily Ma Qadamat wama Akharat - Ya Allah Nisamehe kwa yaliyotangulia na na yatakayofuatia.
Wama Asrarta wama Aalanta - Ya siri na ya Dhahiri.
Wa Anta aAla Kuli Shay-in Qadir -Na wewe ni mwenye uwezo Juu ya Kila kitu.

Amiin.

Ambapo anasema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaposujudu alikua ni mwenye kusema:**

اللّهُمَّ لَكَ سَجَدْتُ وَبِكَ آمَنْت ، وَلَكَ أَسْلَمْت ، سَجَدَ وَجْهي لِلَّذي خَلَقَهُ وَصَوَّرَهُ وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَه ، تَبارَكَ اللهُ أَحْسنُ الخالِقين

Allahuma Laka Sajadu wa Laka Aslamtu - Ya Allah Hakika mimi Nimekusujudia na Kwako wewe Nimejisalimisha.
Wa Anta Rabbi -Na wewe Ndie Mola wangu.
Sajada Wajhi liladhii Khalaqahu - Nimeusujudisha Uso wangu kwa yule alieuumba.
Wa Sawwarahu - Na Akaupendezesha Kimaumbile.
Wa Shaqqa Sama'hu wa Bassarahu - Na Nimewasilisha Mbele yako Usikivu wake na Uonaji wake Tabaraka Allahu Ahsana Al Khaliqiin - Utukufu Kamilifu ni wa Allah ambae ndie m-bora wa Kuumb*a.' (Sunan An Nasai)*

Na anasema Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kua*: **Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alinifundisha Mimi Dua ya Kusoma katika Sala ambapo aliniambia, Sema:**

اللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْماً كَثِيراً، وَلَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ، فَاغْفِرْ لِي مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ، وَارْحَمْنِي، إِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

Allahuma Inni Dhalamtu Nafsi - Ya Allah Hakika Mimi nimejidhulumu Nafsi yangu.
Dhulman Kathiran - Kwa Dhulma Kubwa Sana.
Wala Yaghfiruu Al Dhunuuba Ila Anta - Na Hakuna anaesamehe Dhambi Ila Wewe.
Fa-ighfir Li Maghfiratan Min In-dika - Hivyo Nisamehe Kutokana na Msamaha wako.
Wa Arhamni - Na niingize kwenye Rehma zako.
Innaka Anta Al Ghafuru Al Rahiimu - Kwani kwa Hakika Wewe ni Mwingi wa Kusamehe na Kusitisha Madhambi na ni Mwingi wa Huruma.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo hii Dua aliyofundishwa Abu Bakar As Siddiq *Radhi Allahu Anhu na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua aombe ndani ya Sala yake Iwe ndani ya Rukuu au Sujud au Baada ya At Tahiyyat ya mwisho ni Dua kubwa sana.

Na hii ni kwa sababu Kimaumbile kutokana na Udhaifu wetu Ibn Adam basi hakuna asiekua ni mwenye kukosa kufanya Dhambi iwe kwa makusudi au kwa kughafilika,Hivyo Dua hii inampelekea Ibn Adam kua Mnyenyekevu mbele ya Mola wake kutokana na kasoro na makosa yake na hivyo kua ni mwenye kuomba msamaha.

Kutokana na kujua na kukubali Uwezo Mkubwa wa Mola wake mbele yake, na hivyo Kiumbe husika hua hana kwa kukimbilia katika kuomba Msamaha isipokua kwa Mola wake ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* huku kiumbe husika akiaa ni mwenye kukiri na kukubali kua hakuna atakaeweza kumsamehe na kumhurumia isipokua yule ambae ni mwingi wa Usamehevu na Mwingi wa Huruma na Upole ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* pia kua:

اللَّهُمَّ اغْفِر لِي ذَنْبِي كُلَّهُ دِقَّهُ وَجُلَّهُ وَأَوَّلَهُ وَآخِرَهُ وَعَلاَنِيَتَهُ وَسِرَّهُ

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba katika Sujud kwa maneno yafuatayo:**
***Allahuma Ighfirli Dhanbi Kullahu* - Yaa Allah nisamehe Dhambi zangu zote.**
***Diqqahu wa Jallahu* - Ndogo na Kubwa.**
***Awwalahu wa Akhirahu* - Za Awali na za Mwishoni.**
Wa Aalaniyatu wa Sirru* - Za dhahiri na za Siri.(Sahih Muslim)*

Kwani anasema Imam Al Shafi Al Thani Hujjat Ul Islami, Mujaddid Ad Din Zukhruf Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: '**Fahamu kua Unaposujudu Ndani ya Sala basi hua unakua katika Hali ya Juu kabisa ya Unyenyekevu**. **Na hii ni kwa sababu hua unaiweka chini Ardhini sehemu yenye Thamani kabisa ya Mwili wako, yaani Uso wako**. **Ambapo kuiweka kwako chini huko sehemu hio hua kunakupelekea Muonekano wako huo wenye thamani wa Uso wako kua ni wenye kukutana na kitu kisichokua na thamani kabisa! Yaani Vumbi la Ardhini.'**

Hivyo inavyotakiwa basi kua ni vizuri zaidi Mtu Usujudu moja kwa moja juu ya Ardhi tupu isiyotandikwa kitu juu yake. **Ambako hukupelekea Mtu kua ni mwenye kujihisi kua ni mwenye Unyenyekevu zaidi na hivyo hua ni kuonesha namna Unavyoishusha Thamani na kuidhalilisha Nafsi yako katika wakati huo unapokua kwenye Sujud. Na unapojishusha chini kuingia kwenye Sujud na kusujudu basi Iambie Nafsi yako kua hii ndio asili yako ya kimaumbile.'**

'Na katika kufanya kwako hivyo basi Mtu ndio unakua unajumuisha na kushikamanisha moja kwa moja Tawi kwenye Mzizi wake. **Kwani kwa Hakika Ibn Adam ameumbwa kutokana na Udongo na marudio yake ni katika Udongo.'**

Kwani Hujjat Ul Islami Imam Al Ghazali anaendelea kutuambia kua: '**Wakati ukiwa katika Hali hio ya Sujud: 'Basi Ndio Unatakiwa sasa Uziamshe Hisia za Ndani ya Nafsi yako katika Kua na Yaqini juu ya Ukubwa wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kisha ndio unasema:*Subhana Rabbi Al aAla Wabihamdihi* - Utukufu Kamilifu ni wako wewe Mola wangu ambae Shukrani zote zinastahiki juu yake. Utakapofikia katika Hali hii basi utakua ni mwenye kuboresheka zaidi Kihisia ndani ya Nafsi yako.'**

Na hapa sasa Kua na Uhakika na kua ni mwenye Kujiamini katika Kutumainia Kuingizwa kwenye Kupata Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala*. **Kwani Rehma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni zenye Kumwagikia kwa haraka sana kwa wale waliokua dhaifu na waliojishusha chini kiunyenyekevu. Na wala haziwamwagikii wale ambao ni wenye Kibri na Kujiona.'***(Ihya Ulum Ad Din)*

Kwani tumetumia Ufafanuzi huu kutoka kwa Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali ambae ni Mtu wa pili Duniani baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kufanyiwa Utafiti

na Watafiti wa Ilm mbali mbali katika vyuo vikuu tofauti Duniani kuhusiana na Maisha yake na Ufaham wake Ukubwa wa Ilm yake, hadi akaitwa Hujjat Ul Islami, Imam ambae anakubalika na Madhhab yote ya Kiislam, na nikisema yote basi namaanisha ya Watu wote Wanaosali na Kuelekea Katika Kibla cha Al Kaabah, katika Mji Mtakatifu wa Makkah.

Na Nadhani kama kweli Tutakua Tunasujudu katika Sala zetu kisha tukajihisi kama tunavyotakiwa kujihisi kama aliyoielezea Hujjat Ul Islami Imam Al Ghazali, kisha Tukafanya Tasbih na Kuomba Dua, basi bila ya shaka, Dua hizo lazima zitajibiwa. Kwani Hujjat Ul Islami anasema kua: **'*Amesema RasulAllah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Sala si kitu chochote isipokua isipokua ni Unyenyekevu na kujisalimisha mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***(Ihya Ulumu Ad Din).

Ambapo kama alivyosema Imam Al Shafi Al Thani Hujjat Ul Islami, Mujaddid Ad Din Zukhruf Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: '**Ingawa Tasbih 3 hua zinatosheleza lakini vizuri Kwa Mtu Anaesujudu Kuomba Dua, na hivyo kama atakua amesujudu kwa ajili ya Kisomo cha Qur'an basi Aombe kulingana na Maneno ya Aya hio.'**

Na akasema Imam Al Rabii Ibn Sulayman ambae ni Mwanafunzi Mahiri wa Imam Al Shafii kua: '**Al Shafii alinifahamisha mimi kua: Amesema Sufyana Ibm Uyaynah kua alitufahamisha sisi kua Amesema Ibn Najih kua amesema Mujahid Ibn Sulayman kua:Mtu aliekua Karibu zaidi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni yule aliekua katika Sujud.'**

Imam Al Rabbi Ibn Sulayman anaendelea kutuambia aliyoyasema Imam Al Shafii kua: '**Hakika mimi Najua aliyoyasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo Mimi napenda kua Mtu anaposujudu basi na aseme *Subhanah Rabbi Al Aala Wabihamdihi* mara tatu na kisha aseme aliyoyasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* (Kwa Kuomba Dua) katika Sijda zake huku akiwa anataraji Kujibiwa, wakati Mtu huyo akiwa si Imam'***(Kitab Al Umm)**

Kwani Imam Al Shafii ameweka Sharti la Mtu husika kupendekezwa kuomba Dua katika Sijda kua ni Kutokua Imam.

'Yaani Ni vizuri Mtu kusoma Dua katika Sijda wakati akiwa katika Sala ya Peke yake na hii ni kwa Sababu kama akiwa Imam na kisha akakaa mda mrefu kusoma Dua kwenye Sijda basi hua ni mwenye Kuwapa Uzito Maamuma wake.Na kama Akiwa Maamuma basi huenda Dua yake hio ikampelekea Kuhitilafiana na Imam wake, kama alivyofafamua zaidi Imam Al Shafii katika Kitabu Al Umm.'

Na Mtizamo huo wa Imam Al Shafii pia ndio Mtizamo wa Imam Ibn Aabidin Al Shami Al Hanafi katika Hashiah yake na pia Imam Ali Shurunbulali Al Hanafi katika *Imdad Al Fatah.*

Ambapo hata hivyo Mtizamo huu wa Imam Al Shafii na Imam Ibn Abidin Al Shami Al Hanafi na Imam Al Shurunbulali Al Hanafi ni Mtizamo ambao unapingana kwa Upande wa Wanazuoni wengine wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik kwa mfano Imam Al Zaylai Al Maliki, Imam Al Haskafi Al Hanafi, Imam Al Sarkhasi Al Hanafi n.k

Basi wao wanasema kua: '**Ama kuhusiana na Kuomba Dua ndani ya Sujud ya Sala basi Hadith zinatuonesha kua Mtu anatakiwa kufanya Hivyo katika Sala za Sunna tu na wala si katika Sala za Fardhi . Kwani Sala zote za Fardhi zinatakiwa kusaliwa kama vile ambavyo alivyozisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kutimiza Sunna zote bila kuongeza Ziada, Hivyo ni kwenye**

Sala za Sunnah tu ndio ambamo Mtu anaruhusika kurefusha Sala na kuomba atakavyo(*Al Mabsut, Al Tabyin Al Haqaiq, Dur Al Mandhur)*

Ama tunapozugumzia kuhusiana na Dua katika Rukuu basi tunaona uhimu wake zaidi pale tunapomuangalia Miongoni mwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* aliekua akipendwa sana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikuani Kijana wa Kiansari aitwae Muadh Ibn Jabal *Radhi AllahuAnhu* ambae alisilimishwa na Sahaba Kijana Ambae ndie aliekua Balozi wa kwanza *wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Mji wa Madina aitwae Musab Ibn Umayr *Radhi Allahu Anhu.*

Ambapo baada ya kusilim basi Muadh Ibn Jabar alikua ni Kijana Mwenye Ufahamu mkubwa sana wa Ilm ya Dini ya Kiislam.Kiasi ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimteua kua Balozi wake katika Juueneza na kuufundisha Uislam katika Ardhi ya Yemen.Kwani alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Mwenye Kujua zaidi katika Ummah wangu kuhusiana na Halali na Haram ni Muadh Ibn Jabal'**

Na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alisema pia kua Muadh Ibn Jabal ni kama *Khalillu Allah Ibrahim Alayhi Salam*. Na hivyo siku Moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimshika Mkono Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* na kisha akamwambia kua: **Ewe Muadh Wallahi mimi nakupenda, sanaHivyo Nakushauri Usiwache Kuomba Kila Baada ya Sala kuomba kwa kusema: *Allahuma Aai'ni ala Dhikrika, wa Shukrika, wa Husni Ibadatika* - Ya Allah Nisaidie katika Kukumbuka, Kukushukuru na kukuabudu katika Njia bora kabisa.'***(Imam Abu Daud)*

Ambapo kwa upande mwengine basi Anasema Abu Said Al Khudry *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwambia Muadh Ibn *Jabal Radhi Allahu Anhu* kwa kusema:Ewe Muadh Nakuusia Kua Kila utakapoweka Paji lako la Uso Ardhini kwa ajili ya Kusujudu basi kua ni mwenye kusema:*Allahuma Aai'ni ala Dhikrika, wa Shukrika, wa Husni Ibadatika* - Ya Allah Nisaidie katika Kukumbuka, Kukushukuru na kukuabudu katika Njia bora kabisa.'**

Na hivyo ndivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyomuusia Sahaba wake ampendae.Nasi tunakumbushana na kuhusiana na Kukubalika Kuomba Dua ndani ya Sujud na Umuhimu wake.Kwani tuko katika Kuangalia kuhusiana na Kuomba Dua katika Sujud ambapo anasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad din Imam Abu Zakarriyah Yahya An Nawawi Al Shafii kua: '**Kulingana na Mafundisho ya Madhhab ya Skuli yetu**. **Kuhusiana na Kuomba Dua ndani ya Sujud basi ni kua Inafaa Kuomba ndani ya Sujud ya Sala Juu ya Kila kile kulichoruhusika kuomba katika wakati ambao Mtu anaweza kuomba akismwa nje ya Sala yaani kuhusiana na Maombi ya Mambo ya Kidunia na pia kuhusiana na Mambo ya Kiakhera.'**

Hivyo Inaruhusika kwa mtu kuomba Dua ndani ya Sujud ya Sala kwa kusema kwa Mfano Ya Allah Muokoe Fulani Ibn Fulani kutokana na Kifungo, **Au anaweza Mtu kuomba Apate Mtoto mwema, au Mapato ya Halali, Nyumba nzuri, Mjakazi Mzuri n.k**. **Na Hakuna hata Moja litakalobatilisha Sala yake kati ya Maombi ya Dua hizo kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Skuli yetu (ya Imam Al Shafii). Na Kulingana na Mtizamo wa Imam Malik, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Abu Thawr na Is-haq Ibn Rahawayh basi wao wanasema kuaHaikubaliki Kuomba Dua nyengine yeyote isipokua Dua zilizotajwa ndani ya Qur'an tu.'**

Na Mtizamo wao inaungwa Mkono na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua:Hakika hii ndio Sala yetu, hakuna Maneno ya Watu ndani yake isipokua Tasbih, Dhikr Allah na Kisomo cha Qur'an*(*Sahih Muslim)*

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Lakini kwa Upande wa Skuli ya Madhhab yetu basi Wanazuoni wetu wametumia Uthibitisho wa Kauli ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam pale aliposema:Hakika mimi nimekatazwa kusoma Qur'an katika Wakati ambao nikiwa kwenye Rukuu na Sujud,hivyo Mtukuzeni *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani ya Rukuu na Sujud Zenu, na zidisheni Kuomba Dua ndani ya Sijda kwani Mtajibiwa***(*Sahih Muslim)'*

Kwa hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha Kuombwa kwa Dua ndani ya Sijda bila kuweka Sharti wala kizuizi, na hivyo ndani yake maneno yake haya amejumuisha kila kitu kinachojulikana kua ni Dua. **Na kwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam aliomba Dua mbali mbali katika baadhi ya sehemu za ndani ya Sala,Basi hii inaashiria kua hakuna Ubaya wowote kuomba Dua yeyote Mtu aitakayo.'**

Na tumeona katika Hadith mbili za Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua ameaamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua baada ya Tahiyat ya mwisho kua Mtu achague katika Dua yeyote asome. **Na katika Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* basi tunaona kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema katika Dua ndani ya Sala kua: Ya Rabb Muokoe Al Walid Ibn Walid, Ayyash Ibn Abi Rabbi, Salamah Ibn Hisham na Waliodhulumiwa wote miongoni mwa Waumini**. **Ya Rabb Waimarishie Uwezo kina Mudar na Uwape miaka kama ya Yusuf(Imepokewa na Bukhari na Muslim)**

Na katika Sahihayn *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliomba Dua kwa kusema: Ya Rabb Walaani Waasi waliomuasi Allah na Mtume wakeNa ndani ya Dua hizi mmetajwa Makabila ya Waarabu, na kuna Hadith nyingi zinazofanana na tulizozitaja(*Al Majmuu)*

Naam..hapa inabidi kukumbushana kua kuhusiana na Dua tulizozitaja humu ambazo ni za kiswahili, basi kwa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni kua katika Sala hua haifai kutumia maneno yasiyokua ya Kiarabu, kwani Sala itabatilika kulingana na Mtizamo wa Imam Al Khatib Al Shirbini.

DUA KWA LUGHA ISIYOKUA YA KIARABU NDANI YA SUJUD

❖❖❖

Wanasema Wanazuoni katika Mawsuah Al Fiqhiyyah kua: '**Ama kulingana na Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi hua ni Makruh yaani Inakirihisha na Haipendekezwi Kuomba Dua ndani ha Sala kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu.Na hii ni kwa Sababu Kuomba Dua ndani ya Sala kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu hua ni Kinyume na inavyopendekezwa, na hata hivyo hii hua haimaanishi kua ni Haram.**

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik basi Anasema Imam Al Qarafi Al Maliki kua ni Haram kuomba Dua ndani ya Sala kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu, na hii ni kwa Sababu kufanya hivyo hua ni Kinyume na Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo Imam Al Laqani Al Maliki basi yeye ameifafanua Kauli hii ya Imam Al Qarafi Al Maliki kwa kusema kua:Maana ya Maneno ya Imam Al Qarafi ni kua Kusoma Dua kwa Lugha isiyofahamika hua ni Kinyume na Utaratibu wa Kumtukukuza Allah Subhanah wa Ta'ala na kuonesha Heshima mbele yake.

Imam Al Laqani anaendelea kusema kua: Lakini Kama Maneno ya Dua hio yenye Lugha ya Kigeni kua yanafahamika basi hua inaruhusika kuomba ndani ya Sala na nje ya Sala. **Na hii ni kwa *Sababu Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema katika Kitabu chake kitukufu kua:**

﴿ وَعَلَّمَ آدَمَ ٱلأَسْمَآءَ كُلَّهَا﴾

Wa Aa'alama Adama Asmaa Kullaha -Na akamfundisha Adam Majina ya Kila Kitu*(Surat Al Baqara 2:31)*

Na akasema tena kua:

﴿ وَمَآ أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلاَّ بِلِسَانِ قَوْمِهِ ﴾

Wama Arsalna min Rrasuulin illa bi lisani Qawmihi. - Na Hatukumtuma Mjumbe isipokua kaa Lugha ya watu wake(Surat Ibrahim 14:4)Ambapo Mtizamo huu umenukuliwa kwa Imam Al Dasuqi al Maliki pia

Ama kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii, basi Suali hili limezungumziwa kwa kina kwani Wanazuoni wao Wanasema kua:Ama kuhusiana na Dua zinazoombwa ndani ya Sala basi ziko aina tofauti, kwani kuna ambazo zimenukuliwa kwenye Hadith na ambazo hazikunukuliwa. **Ambapo kuhusiana na Hadith zilizonukuliwa basi juu yake kuna Mitizamo Mitatu:**

Ambapo Mtizamo Unaokubalika zaidi Katika Madhhab ya Imam Al Shafii ni sawa na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Hanbali yaani Inaruhusika Kuomba Dua ndani ya Sala kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu kwa Mtu asiejua Kiarabu. Lakini hairuhusiki kwa Mtu mwenye Kujua Kiarabu, na hivyo Mtu mwenye Kujua Kiarabu Kisha akomba Dua kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu basi Sala yake Hubatilika.

Ambapo Mtizamo wa Pili ni kua Inakubalika Kuomba Dua Ndani ya Sala kwa Lugha ya Kiarabu kaa Mtu anaejua Kiarabu na asiejua Kiarabu.

Mtizamo wa Tatu ni kua Haikubaliki Kuomba Dua Ndani ya Sala kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu, iwe Mtu anaesali anajua Kiarabu au hajui na hii ni kwa Sababu Hairuhusiki Kutumia Lugha isiokua ya Kiarabu ndani ya Sala.'

Al Mawsuah Al Fiqhiyyah Quwaitiya yaani Kamusi ya Fiqh iliyoandaliwa Nchini Quwait inaendelea kufafanua kuhusiana na Suali hili basi inaendelea kusema kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua: '**Ama Kuhusiana na Dua ambazo hazijanukuliwa kutoka katika Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Hairuhusiki Kuvumbua Dua zisizokua katika Lugha ya Kiarabu na hii ni Kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni.'**

'Ama kuusiana na Adhkar nyenginezo kama Tahiyyat ya kwanza, Salat An Nabii, Qunuut, Tasbiih za kurukuu na kusujudu, Takbir za kuhama kutoka katika hatua moja ya Sala kuingia kwenye hatua nyengine ya Sala basi kulingana na mtizamo usemao kua inakubalika kuomba Dua kwa lugha nyengine basi hua pia inaruhusika kutumia Lugha nyengine katika hali ya dharura katika haya, ambapo kuhusiana na kama Mtu anaeruhusika kufanya hivyo ni mwenye kujua lugha ya Kiarabu ama la, basi kuna mtizamo tofauti juu yake'

'Kwani kuna mtizamo usemao kua inakubalika, na kuna mtizamo usemo kua haikubaliki na kunamtizamo wa tatu usemao kua inakubalika lakini kulingana na zile sehemu ambazo kama

ikiwa hayakutamkwa basi inabidi ilipwe fidia ya kuleta Sijda Sahw'*(Al Mawsuah Al Fiqhiyyah Quwaitiya)*

Hivyo hio ni Mitizamo ya Madhhab mbali mbali kuhusiana na Kuomba Dua ndani ya Sala kulingana na Ufafanuzi wa Mkusanyiko wa *Al Mawsuat Fiqhiyyat Al Kuwaytiyyah* ambavyo ni Kama Kamusi la Mkusayiko wa Mitizamo ya Fiqh ya Madhhab tofauti iliyoandaliwa Nchini Kuwayt ambapo Mkusanyiko wake una vitabu 45.

Kwani baada ya kuangalia Mtizamo hio basi na tuangalie moja kwa moja kwenye Mitizamo ya Maimam wa Fiqh wa Madhhab kuhusiana na Jambo hili. Ambapo tunapomkamata Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi basi yeye ansema kua: '**Kusoma Dua ndani ya Sala kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu**. **Hua Kunaruhusika pale inapokua Dua au Dhikr husika hua ni yenye Kukubalika, na hii ni kwa sababu Dua Husika au Dhikr Husika hua Inakubalika Kisharia.Ambapo hata hivyo Kama Mtu atasoma Dhikr au Dua kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu wakati yeye anajua kwa Kiarabu, basi Sala yake Itabatilika**. **Na pia kama Mtu asiejua Kiarabu kisha akatunga tu Dua ya Lugha nyengine basi Sala yake Hubatilika***(Al Minhaj)*

Ambapo kwa upande wa Shaykh ul Islami Imam Al Muhaqqiqin Imam Ibn Hajar Al Haythami Al Makki al Shafii basi na yeye anasema kua: '**Kusoma Dua kwa Lugha isiyokua ya KiarabuHua Kunaruhusika pale inapokua Dua au Dhikr hio ni yenye Kukubalika, ndani ya SalaLakini Kama Mtu atasoma Dhikr au Dua kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu wakati yeye anajua kuisoma kwa Kiarabu, basi Sala yake Itabatilika.Na pia kama Mtu asiejua Kiarabu kisha akatunga tu Dua ya Lugha nyengine basi Sala yake Hubatilika'***(Al Tuhfa)*

Ambapo hua pia ndio Mtizamo wa Imam Abu Amr Uthman Ibn Abd Rahman Salah Ad Din Al Kurdi Al Sharhazuri Al Shafii kama alivyosema Imam Abd AlHameed AlSherwani kua maneno yasemayo "**Na pia kama Mtu asiejua Kiarabu kisha akatunga tu Dua ya Lugha nyengine basi Sala yake Hubatilika**, **yanamaanisha kua maneno ya Dua hio kua si kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kama alivyofafanua Al Kurdi.'***(Hashiyyah Al Shirwani)*

Ambapo kwa Upande wa Al Muhaqqiq Al Faqih Imam Ibn Abidin Ash Shami Al Hanafi basi yeye anasema kua: '**Inaruhusika Kuomba Dua kwa Lugha Isiyokua ya Kiarabu kwa Mtu asiejua Kiarabu, lakini pale inapokua Dua hizo zimetajwa kwenye Qur'an na Sunnah na Maombi ambayo huwezi Kumuomba Mt**u'*(Radd Al Mukhtar)*

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Abu Hanifa kama ilivyotajwa katika Nur Al Iddah. Na kwa upande wa Imam Abu Yusuf na Imam Muhammad Ash Shaybani basi wao wanasema kua: '**Inaruhusika Kuomba Dua kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu ndani ya Sala ikiwemo kwenye Sujud.'**

Na Imam Wahba Al Zuhayly basi yeye anasema katika M*awsuat Al Fiqh Al Islami wa Adilat* kua: '**Kuomba Dua ndani ya Sala kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu kwa Maombi yanayofanana na Mazungumzo na Ibn Adam mwenzako hua ni Makruh Takrim.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Khatib Al Shirbini yeye amesema kua: **'Kuomba Dua ndani ya Sala kusikokua kwa Lugha ya Kiarabu hua Kunabatilisha Sala' *(Al Mughni Al Muhtaj)***

Na kwa Upande wa Shaykh Ibn Taymiyyah basi yeye anasema kua: '**Ama kwa yule anaemuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Ikhlasi basi hua ni mwenye kusikiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* iwe anaomba kwa Kiarabu ama la***(Fatawa Al Kabir)* Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Masalafi.

Kwa Maana hio basi kuna Umuhimu mkubwa sana wa Kujifunza Baadhi ya Dua ili mtu usijue kwa Lugha ya Kiarabu. Na hii ni kwa sababu mbili kwanza kufanya hivyo hua ni Kufuata Sunnah ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama alivyowaonesha kwa Mfano wa Namna ya Kusali kwa Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum*na kisha akawaambia kua Salini kama mlivyoniona nikisali.

Na pili ni kwa sababu miongoni mwa Masahaba walikuwepo pia wasiokua Waarabu kama Suhayl Al Rumi *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua ni Mrumi Au Salman Al Farsy*Radhi Allahu Anhu* ambae alikua na asili ya Kiajemi n.k

Ambapo wote hawa walikua wakisali na kuomba Dua ndani ya Sala zao kwa kutumia Lugha ya Kiarabu Hivyo kama Hujui Kuomba Dua yako uitakayo na inayokubalika kwa Lugha ya Kiarabu basi inaruhusika Kuomba Kimoyo moyo kwa Lugha yako lakini kama Muislam basi unatakiwa ujue kuomba Dua kwa Lugha ya Kiarabu.

Naam..hivyo tunapoangalia Kuhusiana na Dua ndani ya Sujud na sehemu nyengine za Sala na hata nje ya Sala pia basi tunaona kua Hukmu yake katika Kusomwa kwake imegawika katika Hali Tatu kulingana na Hali ya Mazingira ya Mtu husika, mazingira ambayo yamegawika sehemu 3:-

Kwanza kuna hali ya Mazingira ya Mtu kua ni Muarabu aliezaliwa kwenye Mazungira ya Kiarabu na hivyo Lugha ya Kiarabu ndio Lugha yake ya Asili na anaijua Ndani nje. **Hivyo Hukmu ya Mtu kama huyu basi ni kua : Hairuhusiki kwake kuomba Dua ndani ya Sala kwa Lugha nyengine isiyokua ya Kiarabu**. **Kwani hua Inakirihisha sana kwake yeye kuomba Dua kwa Lugha isiyokua ya Kiarabu ndani ya Sala Tuseme labda kwa Mfano haukupita Mda mrefu tangu awe amesilimu, au labda Ni Muislam lakini Hakusoma.**

Basi Hukmu ya Mtu mwenye hali ya mazingira hii ya Tatu, basi kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni tunaona kua Hua Inaruhusika kwao wao Watu wenye hali kama hii ya Kimazingira kuomba Dua kwa Lugha yao. **Na hii ni kwa sababu Maombi ya Dua hua yanatakiwa kua ni yenye kutokea Moyoni.**

Na hivyo ndani yake hua kunahitajika Khushuu na Unyenyekevu na kutokana na kua Mtu husika hajui Lugha ya Kiarabu basi kwake yeye itakua vigumu kuipata hali ya Khushuu na Unyenyekevu kwa sababu ya tatizo la Ugumu wa Kuyatafuta maneno ya Kiarabu ya Dua husika na kisha kuyatafsiri katika Lugha yake na kuyasema kwa Kiarabu na hivyo Moyo wake utashughulika na akili yakena akili itashughulika katika Kutafuta kumbukumbu ya Msamiati na kuachana na Mola wake.'

Hivyo kutokana na Uzito na ugumu huo basi ndio maana akasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua:

وذكر صاحب الحاوي أنه إذا لم يحسن العربية أتى بكل الأذكار بالعجمية

'**Amesema Muandishi wa Al Hawi (Al Qadhi, Al Faqih Imam Al Ibn Muhammad Al Mawardi) kua:Kama ikiwa Mtu hajui Lugha ya Kiarabu basi anatakiwa aombe Dua zote kwa Lugha anayoiju**a.'(*Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Bahadir Al Zarkashi kua: '**Ikiwa Mtu hajui Lugha ya Kiarabu basi ni bora kwake kuomba Dua kwa Lugha**

anayoijua. **Kwa sababu ya Umuhimu wa Kujua maana iliyomo katika Maombi ya Ibada husika,kama Dua zinazopendekezwa kwenye Sala, kwenye Umra kwenye Hajj n.kKwani Mtu atakaposema bila kufahamu hua ni mwenye kuweza kufanya Makosa makubwa ndani ya maombi yake bila ya kukusudia, hivyo bora kwao wao watu hao kusema yale wanayoyaelewa na yale wasiyoyaelewa basi wasome kwa Lugha ya**o.'*(Al Madhur)*

Kwani amesema Allah Subhanah wa Ta'ala katika Kiyabu chake kitukufu kua:

﴿ فَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ مَا ٱسۡتَطَعۡتُمۡ وَٱسۡمَعُواْ وَأَطِيعُواْ وَأَنفِقُواْ خَيۡرٗا لِّأَنفُسِكُمۡ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفۡسِهِۦ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ﴾

Faittaqoo Allaha ma istataAAtum waismaAAoo waateeAAoo waanfiqoo khayran li-anfusikum waman yooqa shuhha nafsihi faola-ika humu almuflihoona*(Surat At Taghabun 64:16)*

Tafsir: ***Hivyo Muogope Na Tekeleza Majukumu yako juu yake kwa Kadiri UtakavyowezaNa Msikilizeni Mtiini na ToeniKwani Kufanya Hivyo ni Bora kwa Nafsi zenu Na Atakae Okoka kutokana na Matamanio ya Nafsi yake Basi Hao ni Miongoni mwa waliofuzu.***

Naam hii ni miongoni mwa aya ambazo Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii amesema kuhusiana nazo kua: '**Ni Moongoni mwa Aya 8 za Surat At Taghabun ambazo ni zenye Lulu za Qur'an.'**

Na bila ya shaka ukiiangalia Tafsiri yake basi utaona kua Hujjat ul Islami hajakosea kutoa Hukmu hio Juu ya Aya hii.

Ambapo mbali ya Aya hii kua na sifa hio lakini pia Aya hii ni yenye sifa ya kua ni Moja kati ya Aya nazo zinatumiwa na Wanazuoni katika Kuthibitisha Kubaliko la Mtu asiejua Kuomba Dua kwa Lugha ya Kiarabu kua ni Mwenye Kuruhusika kuomba kwa kutumia Lugha aijuayo. Na hii ni kwa Sababu Aya imeruhusu kwa Kila Mtu Kumcha *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Kadri awezavyo.

Na uthibitisho huu wa Aya hii unatumiwa katika Mitizamo ya Wanazuoni wengi sana katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa, baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, wengi Miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na pia Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal n.k

Na hivyo kumruhusu Mtu asiejua Lugha ya Kiarabu kuomba kaa kutumia Lugha yake, ambapo hapo hapo Mtu huyo anatakiwa Afanye Jitihada ya Kujifunza Maneno ya Kiarabu ya Dua husika katika wakati wa Sala yake.Ambapo akishajua tukuomba au kusoma kwa Kiarabu basi hua tayari haruhusiki kutumia Lugha nyengineyo zaidi ya Kiarabu.

Kwani Tayari hua ni Mtu ambae amekosa Sifa ya Kutoruhusika kutosoma kwa Kiarabu na hivyo akisoma kwa Lugha yake basi Sala hubatilika.Na hivyo kumruhusu Mtu asiejua Lugha ya Kiarabu kuomba kwa kutumia Lugha yake, ambapo hapo hapo Mtu huyo anatakiwa Afanye Jitihada ya Kujifunza Maneno ya Kiarabu ya Dua husika katika wakati wa Sala yake.Ambapo akishajua tukuomba au kusoma kwa Kiarabu basi hua tayari haruhusiki kutumia Lugha nyengineyo zaidi ya Kiarabu.Kwani Tayari hua ni Mtu ambae amekosa Sifa ya Kutoruhusika kutosoma kwa Kiarabu na hivyo akisoma kwa Lugha yake basi Sala hubatilika.

Ambapo anasema Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki kua: **'Kama ikiwa Dua na Dhikr husika ni zenye hali ya kuFardhi shwa kusomwa ndani ya Sala basi hua hairuhusiki kuzitamka kwa Lugha nyengine. Bali zinatakiwa kutamkwa kama kama zilivyoelezewa kwa Lugha ya Kiarabu kwa mfano Dua na Dhikr zinazosomwa Katika Sijda na baada ya** Atahiyyat **ya mwisho basi hua ni bora kuzisomakama ilivyoelezewa na *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kwa lugha ya Kiarabu.**

Na haipendezi kuzitafsiri hususan katika Sala za Fardhi , ambapo katika Sala za Sunnah, Katika Sala za Usiku, n.k basi hua Inaruhusika Kuziomba kwa Lugha yake Mtu husika, kwa sababu itakua rahisi kwake kuonesha Unyenyekevu.

Ama kuhusiana na Dua na Dhikri zilizoFardhi shwa katika Sala za Fardhi basi Mtizamo uliokua Sahih ni kua inakubalika kuzitafsiri katika Sala lakini hata hivyo Mtu husika anatakiwa ajitahidi kuzitamka na kuzifaham kwa kutumia Lugha ya Kiarabu*(At Tamhiid Sharh Malik Muwwata)*

Na anasema Imam Hasan Ibn 'Ammar Ibn 'Ali Al Shurunbulali Al Hanafikua: **'Kusoma Dua kwa Lugha nyengine hua inakubalika kama mtu akiwa hajui Lugha ya Kiarabu, na hivyo kama Mtu atakua anajua Lugha ya Kiarabu basi hua hairuhusiki kwake kutumia Lugha Nyengine na hio ni kuligana na mtizamo unaokubalika nawengi zaidi'**

Hivyo inabidi tufahamiane vizuri Zaidi basi inabidi tufahamishane kua kuna mambo kadha wa kadha yanaashiria kujuzu kwa dua katika lugha isiyokuwa Kiarabu wakati wa Sala.

Kwanza - Dua katika sala si nguzo wala si Fardhi ya Sala. Ni wajibu kutumia lugha ya Kiarabu kwa hakika, kumekuwa na tofauti katika kusoma Qur'an na dua nyinginezo kwa lugha isiyokuwa ya Kiarabu kwa wale wasioweza kuisoma, hivyo ikapendeza kusema hivyo. dua kwa lugha ya Kiarabu inafaa.

Pili - Hakuna ushahidi wa mtazamo wa uharamu walionao akina Maliki ila kwa mtazamo kwamba dua kwa lugha isiyokuwa Kiarabu inapingana na utukufu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* , na hii ni kauli iliyokataliwa. Kwa sababu Muislamu anatakiwa kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* , na Mwislamu anaweza kuwa Mwarabu au akawa si Mwarabu, na kuweka mipaka ya kutukuzwa kwa lugha ya Kiarabu kunawawekea vikwazo watu, na inadaiwa kuwa kumtakasa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kunatokana na Waarabu tu na si Waislamu wengine. na imejulikana kuwa miongoni mwa wasiokuwa Waarabu wapo wanaomcha *Allah Subhanah wa Ta'ala* zaidi na wapo zaidi kwenye nyoyo za Waarabu wengi, na ulimi haukuishia katika kumwabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Hakika Maliki waliokataza kuomba kwa lugha isiyokuwa Kiarabu waliweka sharti kwamba muombaji asiwe mjuzi wa maana ya dua hiyo. dua. Ni halali Kusali kwa lugha isiyokuwa Kiarabu kwa mujibu wa akina Maliki. Kulingana na Skuli ya mawazo ya Hanafi, haipendezi.

Tatu - *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndiye Muumba wa lugha zote, hivyo Kusali kwa lugha isiyokuwa Kiarabu hakupingani na utukufu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala*, wala hakupunguzii uwezo wa asiekua Muarabu wa kumtukuza, kumsifu na kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni miongoni mwa sheria za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusu uumbaji wake, kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* :

﴿وَمِنْ آيَاتِهِ خَلْقُ ٱلسَّمَاوَاتِ وَٱلأَرْضِ وَٱخْتِلاَفُ أَلْسِنَتِكُمْ وَأَلْوَانِكُمْ إِنَّ فِي ذٰلِكَ لآيَاتٍ لِّلْعَالِمِينَ﴾

Wamin ayatihi khalqu alssamawati waAl ardhi waikhtilafu alsinatikum waalwanikum inna fee dhalika laayatin lilAAalimeena*(Surat Ar Rumi 30:22)*

Tafsir: ***Na miongoni mwa ishara zake ni kuumba Mbingu na Ardhi na tofauti ya Lugha zenu na Rangi zenu hakika katika haya kuna dalili kwa Walimwengu.***

Na akasema tena *Allah Subhanah wa Ta'ala kua:*

﴿وَعَلَّمَ آدَمَ الْأَسْمَاءَ كُلَّهَا﴾

WaAAallama adama Al asmaa kullaha*(Al Baqarah: 31*

Tafsir: ***Na akamfundisha Adam majina ya kila*** kitu.

Nne - Kuna maafikiano juu ya kuruhusiwa kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa lugha isiyokuwa Kiarabu katika nyakati zisizokuwa za sala. Yaani Inafaa kwa asiekua Muarabu Kusali kwa lugha isiyokuwa Kiarabu. Kwa kuzingatia hali ya awali.

Tano - kwamba Uislamu ndio Muhuri wa Utume, na *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* ni Muhuri wa Manabii na Mitume, na kwamba ulitumwa kwa watu wote bila ya kujali Lugha zao na rangi zao, kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَمَآ أَرْسَلْنَاكَ إِلاَّ كَآفَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيراً وَنَذِيراً وَلَكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لاَ يَعْلَمُونَ﴾

Wama arsalnaka illa kaffatan lilnnasi basheeran wanadheeran walakinna akthara alnnasi la yaAAlamoona*(Surat Saba 34:28)*

Tafsir: ***Na hatukukutuma ila uwe Mjumbe Kwa watu, kuwabashiria na kuwaonya lakini wengimiongoni mwa watu si wenye kujua juu ya hilo.***

Na amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kama ilivyosemwa katika Sahih al Bukhari kua:

وكان النبي يبعث إلى قومه خاصة، وبعثت إلى الناس عامة''، وفي رواية مسلم

Na Nabii alitumwa kwa watu wake makhsusi, na mimi nilitumwa kwa watu kwa ujumla,

Na katika Sahih Muslim:

وبعثت إلى كل أحمر وأسود

"Na nilitumwa kwa kila Mtu Mwekundu na Mweusi.

Hivyo Uislamu sio dini ya Waarabu peke yao, bali ni dini ya ulimwengu wote kwa watu wote, na sharti la Kiarabu lazima liwe na mipaka kwa kile kilichomo ndani ya maandishi, na hii inatumika kwa Qur'an tu, kwa sababu Qur'an ni Kiarabu na kuandika maana zake au kuifasiri haizingatiwi kuwa ni Qur'an.

Sita - Sharti la kuomba kwa Kiarabu ni kuweka aina ya ugumu wa maisha kwa watu. Na Ugumu huondolewa katika Sharia kwa maandiko ya Qur-aan na Sunnah, mpaka lengo la kuondoa dhiki na Kuondoa dhiki ndio miongoni mwa malengo muhimu zaidi ya Sharia, kama katika kauli yake *Allah Subhanah wa Ta'ala*

﴿لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا﴾

La yukallifu Allahu nafsan illa wusAAaha*(Surat Al baqara 2:286)*

Tafsir: ***Haikalifishi Allah Subhanah wa Ta'ala Nafsi isipokua kwa Uwezo wake.***

Na kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala :*

﴿مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ حَرَجٍ﴾

Ma yureedu Allahu liyajAAala AAalaykum min harajin(Al Ma'idah: 5:6)

Tafsir: ***Hakutakieni Allah Subhanah wa Ta'ala kukujaalieni Ugumu***"

Na pia katika aya nyengine kua"

﴿وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ﴾

Wama jaAAala AAalaykum fee alddeeni min harajin*(Al Hajj: 22:78)*

Tafsir: ***Na Hajakujaalieni Allah Subhanah wa Ta'ala katika Dini yaliyo Magumu.***

Na pia akasema

﴿يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ﴾

Yureedu Allahu bikumu alyusra wala yureedu bikumu alAAusra*(Surat Al Baqara 2:185)*

Tafsir: ***Anataka Allah iwe rahisi kwenu na wala hataki iwe ugumu kwenu.***

Na akasema pia:

﴿يُرِيدُ ٱللَّهُ أَن يُخَفِّفَ عَنْكُمْ وَخُلِقَ ٱلإِنسَانُ ضَعِيفاً﴾

Yureedu Allahu an yukhaffifa AAankum wakhuliqa Al insanu dhaAAeefan*(Surat An Nisaa 4:28)*

*Tafsir:****Anataka Allah kukurahisishieni juu yenu, kwani amemuumba Mtu kua Dhaif.***

Ambapo Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Musa Al Shatibi Al Andalus Al Malik iambae ni Mtaalam mahiri sana wa Ilm ya Maqasid Al Shariyah yaani Ilm yenye kufafanua Malengo ya Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi amesema kua:

وفي الحديث: بعثت بالحنيفية السمحة. وما خير بين شيئين إلا اختار أيسرهما ما لم يكن إثما، وإنما قال: ما لم يكن إثما لأن ترك الإثم لا مشقة فيه من حيث كان مجرد ترك، إلى أشباه ذلك مما في هذا

المعنى، ولو كان قاصدا للمشقة لما كان مريدا لليسر ولا للتخفيف، ولكان مريدا للحرج والعسر وذلك باطل."

"Na katika Hadithi: Nimetumwa pamoja na kua na Hanifiyyah Mvumilivu. Hakupewa chaguo baina ya mambo mawili isipokuwa alichagua lililo jepesi zaidi katika mawili maadamu si dhambi. kuachwa tu, na kitu kinachofanana na hicho katika maana hii, kama angekusudia ugumu, asingetaka urahisi au aibu, na hiyo ni batili.*(Al Muwafaqat)*

Hivyo Kikanuni katika sheria ya Fiqh hua ni kuwahimiza Waumini kuomba Dua mara kwa mara wakati wakiwa ndani ya Sala, Hivyo kama ikiwa sio Waarabu na lazima kuomba kwa lugha ya Kiarabu, basi itakua ni vigumu kwao kuomba wayatakayo ndani yake, na hivyo hii hua inapingana na malengo ya Sala.

Saba - Lugha ni chombo na njia ya mawasiliano katika kuainishamalengo ya Ibn Adam katika Maombi yake mbele ya*Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae anajua na kusikia na kufahamu Lugha za viumbe wake wote.

Nane–na kama ikiwa Sharti la lugha ya Kiarabu katika kuwaombea wasiokuwa Waarabu; basi hii inaashiria kua Uislamu unapendelea Waarabu juu ya wengine, na kanuni ya msingi ni kwamba Waislamu ni sawa mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kusema kwamba inafaa Kuomba Dua kwa lugha isiyokuwa Kiarabu kunaongeza mafungamano yanayowaungaunisha Waislamu wasio Waarabu na Uislamu, na ni moja ya madhumuni muhimu ya sheria ya Sharia.

Tisa - Usisitizaji wa kuhitajika kwa lugha ya Kiarabu katika Dini ya Kiislam ulisababisha baadhi ya Waislamu kuunda uzushi. Ikiwa mtazamo wa uwezeshaji unapingana na uvumbuzi na kuuzuia, basi taarifa na upendeleo wake sio sahihi zaidi.

Kumi - Kauli ya kwamba dua inafaa kwa lugha isiyokuwa Kiarabu ni rai ya mtizam unaokubalika na Wanazuni wengiesana wa Fiqh katika uchunguzi, hata kwa wale wanaojua vizuri Kiarabu.

Amesema Abu Said Al Khudry *Radhi Allahu Anhu* kua**: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua; Hakuna Muislam ambae Atakaeomba Dua ambayo haina Dhambi Ndani yake wala Yenye Kuvunja Udugu ndani yake isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamjibu kupitka katika moja kati ya Njia Tatu zifuatazo:**

1-Aidha Dua yake hio Itajibiwa Haraka Sana.

2-Au Dua yake hio Itahifadhiwa hadi Siku ya Malipo na Kujibiwa.

3-Au Ataepushwa Na Ovu kulingan na Dua yake hio.

Masahaba *Radhi Allahu Anhum*wakasema: Basi Kama ni Hivyo *Ya Rasul Allah,* Na tuombe mara kwa mara Zaidi.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu : Allah ni Mwenye Wingi wa Umiliki Zaidi.'(Musnad Imam Ahmad, Mustadrak Al Hakim)*

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

خطبَنا رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليهِ وسلَّمَ ، فقال : أيها الناسُ . . قد فُرِضَ عليكم الحجُّ فحُجُّوا ، – فقال رجلٌ : أكُلَّ عامٍ يا رسولَ اللهِ ؟ فسكتَ حتى قالها ثلاثًا . فقال رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليهِ وسلَّمَ : لو قلتُ : نعَم ، لوجبَتْ ولما استطعتُم ، ثم قال : ذَروني ما تركتُكم ، فإنما هلك من كان قبلَكم بكثرةِ سؤالِهم واختلافِهم على أنبيائِهم ، فإذا أمرْتُكم بشيءٍ فأْتُوا منه ما استطعتُم ، وإذا نهيتُكم عن شيءٍ فدَعُوه

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema: 'Enyi Watu! Ibada ya Hija imeFardhi shwa kwenu hivyo Fanyeni Ibada ya Hija, Ambapo Kuna Mtu akauliza:Jee Ni Kila Mwaka ya Rasul Allah? Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakujibu, na hivyo Mtu huyo akauliza hadi ilipofikia Mara ya Tatu. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Kwa Hakika kama ningejibu Ndio basi Ingekua ni Wajibu. Kwenu Kuhiji Kila Mwaka, Na nyinyi Msingekua na Uwezo huo, Hivyo Msiniulize kuhusiana na kile ambacho sijakibainisha.**

Kwani Watu waliotangulia Kabla yenu Waliangamizwa kutokana na Kuwahoji sana Mitume wao na Kupingana nao, Hivyo kama nikikuamrisheni kitu basi Kitekelezeni kwa Kadri ya Uwezo wenu. Na nikikukatazeni basi Achaneni nacho.'*(Bukhari na Muslim)*

Hivyo katika Kuangalia kuhusiana na Dua Katika Sijda na Kuruhusika kwake kuomba Dua kwa Lugha Nyengine. Ambapo kama tulivyoona kua Wengi Miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua Inakubalika na kuna baadhi Wasemao kua Haikubaliki. Na tunaangalia Hadith hizi mbili kwa sababu ndani yake Hadith hizi zina mafunzo Makubwa sana.

Ambapo Katika Hadith ya kwanza basi tunaona kua Ingawa inaruhusika Kuomba Dua kwa Lugha nyengine zaidi ya Kiarabu Ndani ya Sala kwa wasiojua Lugha lakini hata hivyo Maombi ya Dua hizo hua yana Mipaka yake, kwani Kuna Dua ambazo hazikubaliwi hata uwe unajua Kiarabu, wacha mbali ukiwa Hujui.

Ambapo miongoni mwa Mifano ya yasiyokubaliwa ni Kama ilivyosema Hadith kua Kuomba Kufanya Dhambi, labda tuseme Maombi ya Kutaka Kuzini na Mwanamke Fulani labda, au ya Kutaka Mwenzako aondokane na Nerma aliyojaaliwa na Mola wake kutokana na Wivu wako juu yake. Au labda unataka Kuwatenganisha Ndugu wawili au Wanandoa kutokana na Wivu wako, n.k

Hivyo haya ni Mambo ambayo Hayakubaliki katika Dua husika iwe unajua Kiarabu au Hujui, na Ukiomba Dua kama hio basi Sala yako ni Batili.

Kwani Hadith ya pili inatufunza Kuachana na Mambo yaliyokatazwa ikiwemo yasiyotakiwa kuombwa kwenye Dua kama ilivyosema Hadith ya kwanza.

Kisha Hadith ya pili pia inatuonesha kua Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* hua yanatakiwa kutekelezwa kulingana na uwezo wa Mtu.

Kwani hadith hii ndio iliyotoa Kanuni ya Fiqh isemayo kua: '**Hakuna Jukumu juu ya Mtu isipokua Kulingana na uwezo wake'**

Na hivyo basi kutuonesha kua Mtu anaweza kuomba Dua ndani ya Sala kulingana na Uwezo wake kama anajua Kiarabu ataomba kwa Kiarabu kama hajui basi ataomba kwa Lugha yake, muhimu ni kua na Unyenyekevu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kuomba kwake.

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿ وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِى عَنِّى فَإِنِّى قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُواْ لِى وَلْيُؤْمِنُواْ بِى لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ﴾

Wa-idha saalaka AAibadee AAannee fa-innee qareebun ojeebu daAAwata alddaAAi idha daAAani falyastajeeboo lee walyu/minoo bee laAAallahum yarshudoona. *(Surat Al Baqara 2:186)*

*Tafsir:**Na Hivyo Watakapokuulizia Waja wangu Juu yanguBasi Mimi Niko Karibu nao Sana KujibuDua za Muombaji AtakaponiombaHivyo Wacha wasikilize Wito wangu kwa Utiifu Na Waniamini ili Wapate kuongozwa.***

Ambapo Hadithi hii ya pili ni Munasaba kuhusiana na habari ya Funga ya Arafah, pia ambayo ni yenye kutukataza kuhusiana na kuuliza Masuali mengi kwani yatatuangamizisha. Kwani kila mtu anajua kua *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* hakuwahi kufuata Muandamo wa Mji wa Makkah katika kipindi cha uhai wake wote alichokua akiishi katika Mji wa Madina.

Halafu leo watu wanaulizana masuali mengi sana kama vile vile alivyokataza *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua Watu wasiulize Masuali mengi. Basi leo wanauliza kwa visingizo kua eti itakuaje wakati ilikua hakuna Televisheni, hakuna Mtandao, hakuna simu, wakati leo Dunia iko kiganjani. *Subhanah Allah!*

Hivi jee kama hizi ni hoja zinazoingia akilini, basi labda tuulizane kua jee *Allah Subhanah wa Ta'ala* alikua hajuia kua baadae katika wakati wetu vitakuwepo viu hivyo? Na hivyo hakuweza kumwambia *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam?*

Ambapo tukuliangalia hili basi tutaona kua bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni *Al Alimun*, Mjuzi juu ya kila kitu tangu kutokuwepo kwake kitu husika, mwanzo wake katika kuwepo kwake baada yake, na mwisho wake kitu husika au tukio husika, kwa sababu yeye ni mwenye kujua juu ya kila kitu na pia ni *Al Hakim* mwingi wa Hikma.

Nakutokana na kua ni mwingi wa Hikma basi ndio maana ikawa katka Hija ya mwanzo mbali ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*hakuenda katika Ibada hio na hivyo Ibada hiyo ikawa ni yenye kuongozwa na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu,* ambapo hata hivyo*Allah Subhanah wa Ta'ala* hakumwambia *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua kesho kina Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kua watasimama Arafah katika Mji wa Makkah, hivyo nawe waambie watu wa Madina waliokua hawajaenda Makkah katika Ibada ya Hija kua kama wanataka kufunga basi na wafunge kesho ili Arafa iendane sambamba na kisimamo cha Mahujaji wa Makkah…Jee kwanini hakumshushia Wahyi juu ya hilo? Au labda watu wanadhania kua*Allah Subhanah wa Ta'ala* hana uwezo huo? Astaghfir Allah!

Hivi Jee Waislam Hamtafakkari? Kwani Jawabu ni kua *Allah Subhanah wa Taala* hakumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Kwa sababu za Yeye ndie Muumba wa Kila kitu na hivyo Anajua kua kila Sehemu ina Muandamo wake kulingana na Wakati wake na ndio maana *akamuachia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* afunge Arafah kwa Muandamo wa Madina na wala si wa Makkah ili mimi nawe kama kweli tunafuata Sunna zake na maamrisho yake basi tufuate Mfano huo kutoka kwake.

Kwani anasema Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Musa Al Shatibi Al Andalus Al Maliki ambae ni Miongoni mwa Wanazuoni wanaoongoza katika fani ya Ilm ya Maqasid Al Shariyah yaani Malengo ya Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Viumbe wake kua:

Amesema *Rasul Allah Salallhu Alayhi wa Salam* katika Hadith kua: Nimetumwa mimi kwa Ajili ya kua na hali ya Muumini wa kweli mwenye Uvumilivu. Ambae anapopewa hali ya kuchagua baina ya hali mbili basi huchagua lililojepesi zaid baina ya mambo husika pale inapokua urahisi huo hauhusishi dhambi ndani yake.

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua Pale jambo jepesi hilo halihusishi dhambi ndani yake kwa sababu hua hakuna Ugumu katika Kuachana na Dhambi, na hii ni kwa sababu kinachotakiwa kufanya ni kuachana nayo tu dhambi husika, na mithali ya vitu kama hivyo kimaana.Hivyo kama ingekua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ajaribu Kuyafanya Mambo yawe magumu basi angeyafanya Mambo yawe magumu kweli na angerahisisha na asingekubalika.' *(Al Muwaffaqat)*

Naam..ufafanuzi huu wa Imam Al Shatibi ni wenye kuweka wazi kua Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yetu hayamaanishi kutuwekea ugumu bali kuturahisishia.Ambapo tunapoangalia ufafanuzi huo basi tunaona kua Kutokana na kua Malengo ya Ibada ni Kurahisisha Ufanywaji wake basi bila ya shaka hata wale wasiojua Lugha ya Kiarabu wakilazimishwa kuomba Dua kwa Kiarabu basi itakua hayafikiwi Malengo ya Sharia juu ya Ibada ya Sala. Kwani itakua kuna Ugumu kwa Wasiojua Lugha ya Kiarabu.

Na mbali ya Hadith hio ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini pia *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwenyewe amesema katika Kitabu chake kitukufu kama tulivyoona katika aya ya 185 ya *Surat Al Baqarah* na katika aya ya 6 ya Surat Al Maidah na tunapoyaangalia maneno ya Hadith na Aya zote hizi basi tunaona kua Mantiki yake ni kua Uislam umerahisisha Kila kitu ili kisiwe kigumu kwa wafuasi wake na hii ni kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mwenye Sifa ya Kua ni Muadilifu.

Na Kila mwenye sifa ya Uadilifu hua si mwenye kua na sifa ya Kuyafanya Mambo yawe Magumu kwani Mambo yakiwa magumu katika Jamno fulani basi watakao nufaika na Jambo hilo watakua ni kidogo sana hata kama wengi wao watataka manufaa hayo, lakini watashindwa kwa Ugumu wake. Lakini kama mambo yakiwa mepesi basi kila Mtu atanufaika na manufaa ya jambo husika. Na hivyo Uadilifu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Waja wake wanaomuamini hua ni wenye. Manufaa ya kuwarahisishia Waja hao katika Kunufaika kiurahisj na Manufaa yaliyomo ndani ya Maamrisho yake

Kwani tunapoziangalia Aya hizi na Hadith na Malengo yake kisharia na Uadilifu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi tunaona wazi kua hata Manufaa ya Funga ya Arafa kwa wasioenda katika Ibada ya Hija yanakua ni rahisi kupatikana na Kila Muumini Ulimwenguni kama itakua kila Muumini Atafunga Funga hio kwa kufuata Muandamo wa Mwezi 9 wa Sehemu aliyokuwepo Kwani tukisema kua Watu wafuate kisimamo basi kuna Watu wa nchi nyengine ambao kamwe hawatowez kukipata Kisimamo cha Arafah kwa sababu kwao wao itakua ni Usiku na tunapozungumzia Ibada ya funga basi sharti lake hua ni kutekelezwa Mchana na sio Usiku.

Na kwa kua watu hao kwao itakua ni Usiku basi itakua vigumu kwao kuweza kutekeleza Ibada hio, na hivyo kwao wao itakua hawakufanyiwa Uadilifu.Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* hana Sifa ya Kutokua na Uadilifu na ndio maana akawa pia hana sifa ya kuwafanyia Ugumu waja wake. Hivyo Uadilifu unaendana na Urahisi na ndio maana Ikawa Kila Mtu afunge kulingana na Mwezi 9 ya Muandamo wa mwezi wa sehemu aliyokuwepo..ambapo kwetu sisi si leo bali ni kesho *In-shaa Allah.'*

Hivyo Wanazuoni Wanakubaliana kua hakuna Ulazima wa Mtu kua anatakiwa kuomba Dua zilizomo ndani ya Qur'an tu au zilizomo ndani ya Sunna tu, kwa sababu kufanya hivyo sio Wajibu. Kitu Muhimu ni kua Katika Kuomba Dua kwake Mtu husika basi anatakiwa ahudhurishe Moyo ambao uende sambamba na yatamkwayo na Ulimi

Na inaruhusika Kuomba Ndani ya Sala kila kitu ambacho Kinaruhusika Kuomba nje yake, na kila kisichoruhusiwa kuombwa nje yake basi hakiruhusiwi pia kuombwa ndani yake

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Burhan Ad Din Abu Hasan Ali Ibn Abdul Jalil Abu Bakr Ibn Khalil Abu Bakr Habib Al Marghinani Al Rashdani Al Hanafi kua: **'Mtu anatakiwa Aombe anavyotaka kunakofanana na Maneno ya Qur'an na Dua za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kisha Chagueni Dua zilizo bora, hivyo Mtu unaanza kwa kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam na familia yake ili kupata Ukaribu wa kujibiwa Dua yako, na hivyo Usiombe kama wazungumzavyo Watu ili usije ukapotea katika Kuomba kwako.'***(Al Hidaya Sharh Al Bidaya)***

Hivyo kila Mti na mapendekezo yake kuhusiana na Shida yake katika anauouahitajia kutoka kwa Mola wake kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Wacha Mtu amuombe Mola wake kwa Kila kitu anachokihitajia, hata kama Nyuzi ya Kiatu pale itakapokatika'***(Sunan At Tirmidhii)*

8-AL I'ITIDAL BAYNA SIJDATAYN

❖❖❖❖

Kwani kama tunakumbuka katika Hadith ya Rifaa Ibn Rafii R*adhi Allahu Anhu* aliesema kuhusiana na Bedui alieingia Msikitini na kisha Akasali katika Kusali kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamrudisha mara tatu kutokana na kukosea kwake na hivyo Bedui huyo akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua bora amfundishe kusali. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia: Unapotaka Kusali basi Tia Udhu kama alivyoamrisha A*llah Subhanah wa Ta'ala,* kisha Adhini na Qimu Sala.

Kisha Ukianza Kusali basi Soma Surat Al Fatiha kama unajua na kama hujui basi Mtukuze *Allah Subhanah wa Ta'ala, Fanya Dhikr Allah na Tahlil.*

Kisha Rukuu hadi uwe umetulia katika Kurukuu kwako, Kisha Simama Sawia, Kisha Sujudu Kikamilifu. Kisha Kaa Kitako hadi uhakikishe Umepimzika, Kisha Sujudu Kikamilifu kisha Simama kikamilifu.

Na ukifanya hivyo basi utakua umekamilisha Sala yako kikamifu, na kama ukiwa umepunguza basi hukukamilisha Sala yako.

Na hivyo ni bora kuliko kutokamilisha kwani ikipungua Kitu Sala yako basi itakupinguzia Malipo yake, ingawa hutokosa kabisa.*(Imam At Tirmidhii)*

Naam...Hadith inatuonesha kua baina ya Sijda Mbili za Rakaa moja ya Sala basi kati kati yake hua kuna Kituo cha kukaa na kutulia baada ya kutoka kwenye Sijda ya kwanza kabla ya kuingia kwenye Sijda ya Pili.

Ambapo Kitendo hiki hua kinafanywa na kutofautishwa kwake kwenye Sala kwa kutumia Takbir Al Itiqam yaani Takbir ya kuhama kutoka kwenye hatua za Sala. Hivyo tukio la mtu anaesali anapotoka kwenye Sijda ya kwanza na kusema Allahu Akbar na kisha akakaa kitako hadi akatulia hua linajulikana kama Al Itidal bayna Sajdatayn yaani I'tidal Baina ya Sijda mbili.

Ambapo neno Al I'tidal maana yake ni kama tulivyosema hapo kabla kua ni Kua na Hali ya Kati na Kati baina ya Hali mbili zinazotofautiana.

Hivyo Tunapozungumzia kuhusiana na Itidal ndani ya baina ya Sujud Sala hua tunazungumzia kitendo cha kutulia baina ya Sijda mbili za Sala ambazo zenyewe hua ni Nguzo ya 7 ya Sala na Itidal yenye baina yake hua ni Nguzo ya 8 ya Sala.

Ambapo hatua hii ya I'tidal hua ni yenye Kuambatana na Kitendo chengine Muhimu ndani yake kinachojulikana kama Jalasa, yaani mkao wa Kukaa Kitako, ambacho nacho huhesabiwa kua ni Nguzo ya Sala pia, na hivyo inabidi tufahamishane kwa umakini ili tuwe ni wenye kufanikisha kikamilifu Sala zetu.

Kwani amesema pia Abu Humayd As Saadi *Radhi Allahu Anhu* kua:

كان رسول الله صلى الله عليه وسلم إذا قام إلى الصلاة يرفع يديه حتى يُحَاذِيَ بهما مَنْكِبَيْهِ ، ثم يُكبِّر حتى يَقِرَّ كل عظم في موضعه معتدلا، ثم يقرأ، ثم يكبِّر فيرفع يديه حتى يُحاذي بهما مَنْكبيه، ثم يركع سمع الله لمن :ويضع رَاحَتَيْهِ على رُكبتيه، ثم يعتدل فلا يَصُبُّ رأسه ولا يُقْنِعُ ، ثم يرفع رأسه، فيقول الله أكبر ثم يهوي إلى الأرض فيُجافي :حمده، ثم يرفع يديه حتى يُحاذي بهما منكبيه معتدلا، ثم يقول يديه عن جنبيه، ثم يرفع رأسه ويَثْني رجله اليسرى فيقعد عليها، ويفتح أصابع رجليه إذا سجد، ويسجد الله أكبر، ويرفع رأسه ويَثْني رجله اليسرى فيقعد عليها حتى يرجع كل عظم إلى موضعه، ثم :ثم يقول يصنع في الأخرى مثل ذلك، ثم إذا قام من الركعتين كبر ورفع يديه حتى يحاذي بهما منكبيه كما كبر عند افتتاح الصلاة، ثم يصنع ذلك في بقية صلاته حتى إذا كانت السجدة التي فيها التسليم أخر رجله صدقت هكذا كان يصلي صلى الله عليه وسلم :اليسرى وقعد مُتَوَرِّكًا على شقه الأيسر، قالوا

Abu Humayd Al Saadi Akasema: '*Rasul Allahu Alayhi wa Salam* anaposimama Kusali, alikuwa akinyanyua mikono yake sambamba na mabega yake, akitamka Takbir, kisha anasubiri mpaka kila mfupa wa mwili wake utulie sawasawa. Kisha alikuwa akiisoma (Qur'ani), kisha anainua mikono yake sambamba na mabega yake na kusema Takbir, kisha akainama, akiweka viganja

vyake juu ya magoti yake, kisha alikuwa akisimama wima akiinamisha kichwa chake bila kukiinua sana kisha anasema: '*Samia Allahu Liman Hamida'* kisha huinua mikono yake hadi usawa wa mabega yake huku akisimama wima Kisha husema Allahu akbar na, huku akiweka mikono yake mbali na ubavu wake, kisha anainua kichwa chake na kunyoosha mguu wake wa kushoto na kuukalia juu yake, na alikuwa akikunjua vidole vyake vya miguu wake wa kulia na hukaa hivyo mpaka kila mfupa urudi mahali pake. Kisha anaposimama baada ya Rakaa mbili, aliinua mikono yake hadi usawa wa mabega yake kama alivyokuwa akifanya mwanzoni mwa Salah. Kisha alikuwa akimalizia sala yake iliyosalia kwa namna hiyo hiyo, na anapofika kwenye sijda inayofuatiwa na Taslim, alisogeza mbele mguu wake wa kushoto na kukaa, huku akiweka makalio yake upande wa kushoto juu ya ardhi." *(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhi)*

Ambapo kwa Upande mwengine basi Imam Ibn Hibban yeye ameinukuu Hadithi hii huku ikiwa ni yenye maneno yasemayo kua: '**Na Hukalia Ugoko wa Mguu wake wa Kushoto katika Hali ya Tawarruk'***(Sunan Al Kubra)*

Naam.hizi ni Hadith mbili ambazo zinamitiazamo tofauti Ambapo mkao wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ulielezewa na Hadith hii ya Imam At Tirmidhii hua Unajulikana kama Mkao wa Iftirash. Yaani Mkao ambao Makalio yanakalia Mguu wa Kushoto ambapo huku Unyayo wa Mguu wa Kulia Ukiwa Umesimama na kupindisha vidole vikiaa vimeelekea Kibla.

Kwani kukaa katika Mkao wa Iftirash baina ya Sijda mbili na baina ya Allahu Akbar mbili hadi Mifupa yako ikatulia sawia hua ni Sunna kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.
Ambapo kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Jalasa yaani Kukaa baina ya Sijda mbili hua ni Nguzo Ndogo miongoni mwa Nguzo za Sala. Na ingawa hua inapendekezwa zaidi kukaa katika Mkao wa Iftirash lakini hata hivyo hua inaruhusika pia kukaa katika Mkao unaojulikana kama mkao wa Iq'a.

Ambapo huu hua ni Mkao ambao Mtu anakalia Visigino huku huku vidole vya miguu yake vikiwa chini na vimeelekea Kibla. Na miongoni mwa Wanaosema kua ni bora zaid kukaa mkao wa Iq'aa basi ni Imam Al Bayhaqi, Imam Al Iyad, Imam Amr Ibn Salah, Imam Ahmad Ibn Hanbal,Imam Kamal Ibn Hummam na Imam Al Shawqani.

Na kama Tulivyoona katika Hadith aliyoinukuu Imam Ibn Hibban yaani yeye amesema Kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikalia Mkao wa Tawarruk, ambao Wanazuoni wa Madhhab Ya Imam Al Shafii wanapendekeza kua Mkao huo hua ni Sunnah kukaa katika Attahiyat ya Mwisho kama tutakavyoona hapo baadae tutakapo zungumzia kuhusiana nayo Inshaa Allah.

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Jalasa (Kukaa Kitako) baina ya Sijda mbili basi kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua kuna Mitizamo miwili juu yakeAmbapo mtizamo wa kwanza ni kua Jalasa hua ni Nguzo ndogo miongoni mwa Nguzo za Sala**. **Kama ilivyoelezewa na Shaykh Abu Muhammad, Imam Al Baghawi na wengineo, na Imam Al Raafi amekubaliana na kuthibitisha juu ya hili**.

Mtizamo wa pili ni ule usemao kua Jalasa Ni Nguzo Kubwa miongoni maa Nguzo za Sala. **Ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Ibn Sura yj na wengi miongoni mwa Wanazuoni**.

Hivyo Kama tukisema kua ni Nguzo Kubwa ya Sala, basi hua inaruhusika Kukirefusha kikao hicho.Na kama tukisema kua Jalasa ni Nguzo ndogo basi hua kuna utofauti wa Mitizamo

kuhusiana na Kukirefusha kwa Makusudi, ambapo hua ni sawa na Mtizamo wa Kuirefuaha Itidal ya Kisimamo baada ya Rukuu.

Ambapo kuhusiana na Itidal basi kuna Mitizamo Mitatu juu yake, ambapo Mtizamo sahih ni Mtizamo wa Imam Al Haramayn Al Juwayn. **Ambao ni kua Kuirefusha Itidal hua kunabatilisha Sala, ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Al Baghawi aliousimamia kwa umadhubuti.**

Mtizamo wa pili ni kua kurefusha Itidal hua hakubatilishi Sala, kwani hii hua ni sawa na Mtu anaeirefusha Rukuu, ambapo huu ni Mtizamo wa Al Qadhi Abu Tayyib Al Tabari, na ameusimamia na kuutetea ipasavyo.

Mtizamo wa Tatu ni ule usemao kua kama Mtu atakua ni mwenye Kusoma Qunut kwa makusudi atakapotoka kwenye Rukuu, na kisha akasoma Qunut katika si sehemu zaidi ya hio ambayo ai sehemu yake basi Sala yake Itabatilika. **Lakini kama atairefusha Itidal si kwa Qunut bali kwa Dhikr Allah basi Sala yake haitobatilika.'**

Hivyokama Mtu atakaa baina ya Sijda Mbili na kuirefusha basi kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni kua Sala ya Mtu huyo itabatilika. Kwani anasema alivyofafanua Imam Al Khatib Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shirbini kua: '**Miongoni mwa Mambo yanayobatilisha Sala hua ni Kuirefusha Nguzo Fupi kwa makusudi, ambayo ni Itidal na Jalasa baina ya Sijda mbili**. **Na hii ni kwa sababu Sehemu hizo hazikukusudiwa kurefushwa kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu na huo ndio Mtizamo unaokubalika Zaidi.**

Ambapo anasema Imam Sulayman Ibn Muhammad Al Bujaraimi basi yeye anafafanua zaidi kuhusiana kutoruhusika kukirefusha kikao cha baina ya Sijda mbili kwa kusema kua: **'Kigezo cha kurefusha Itidal kubatilisha Sala ni kua,Mtu anapotoka kwenye Rukuu, hua ni mwenye kusimama kwa kiasi ya Kusoma Surat Al Fatiha ambako hua. Ni yenye kuchukua Mda zaidi ya Dhikr zinazo ruhusika katika Itidal.**

Na kigezo kinachobalitisha Sala katika Kurefusha Kikao cha Baina ya Sujud Mbili hua ni sawa na Mtu mwenye mda wa Kusoma Attahiyat, jambo ambalo hua ni kuzidisha zaidi ya Mda wa Dhikr za sehemu husika.'

Naam..hio ni kuhusiana na Utofauti wa Mitzamo kuhusiana na Kurefusha Kikao cha baina ya Sijda mbili. Kwani anasema As-hab Al Wujuh Imam Abu Qasim Ibn Muhammad Al Rafii Al Shafii katika Fat-h Al Aziz ambacho ni Ufafanuzi wa Kitabu Cha Fiqh cha Madhhab ya Imam Al Shafii cha Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali kiitwacho Al Wajiz kua: '**Itdal yaani Kusimama baada ya Kurukuu na Jalasa Kukaa Kitako baina ya Sijda Mbili, hua zinahesabika kua ni Nguzo Ndogo za Sala katika Madhhab ya Imam Al Shafii kutokana na kua ni zenye Kutofautisha baina ya Nguzo kubwa za Sala.**

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Hanifa na kulingana na Mitizamo miwili ya Maimam wa Madhhab ya Imam Malik,basi wao wanasema kua Inaruhusika Kutonyanyuka kutoka katika RukuuNa hivyo Mtu anaweza kuenda moja kwa moja kutoka kwenye Rukuu hadi kwenye Sijda,kwani hakuna ulazima huo wa Kunyanyuka'*(Fat-h al Aziz)*

Kwani anasema Imam Said Ba Ishni kua: '**Kulingana na Madhhab yetu ya Imam Al Shafii basi ni kua:Kama mtu atairefusha kwa Makusudi *Itidal* baafa ya Kurukuu au Jalasa baina ya Sijda Mbili, kwa mda wa kiasi ya ukubwa wa Kusoma Surat Al Fatiha au Kusoma Attahiyat ya Mwanzo. Basi Sala ya Mtu huyo Itabatilika lakini pale Mtu huyo anapokua anajua kua**

Kuirefusha huko Itidal au Jalasa kua hua kuna batilisha Sala. **Ama kwa upande mwengine basi Iuna Wanazuoni ambao wana ihesabu Itifal na Jalasakua ni Nguzo ndefu ya Sala.'** *(w*

Na tunaporudi kwa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi basi anasema katika kuifafanua Hadith ya Hudhayfa Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua: '**Usiku mmoja nilisali na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*,na akaanza kusoma*Surat Al Baqara*,na nikadhania Atasoma Aya Mia tu, lakini aliendelea Kusoma na nikadhania kua ataisoma Sura nzima kwenye Raka ya kwanza lakini alipoimaliza akasoma Surat An Nisaa mpaka akaimaliza,na kisha akasoma Surat Al Imran, kisomo chake kilikua ni cha utaratibu na akifika katika Aya yenye kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi husema *Subhanah Allah*.'**

'Akifikia Aya yenye Dua huomba Dua,akifika kwenye Aya yenye kuzungumzia Hifadhi wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi huomba hifadhi. **Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akarukuu na akasema *Subhanah Rabbi Al Aadhiim***. **Ambapo Rukuu yake ilikua ndefu kama Kilivyokua Kisimamo chake, na kisha akanyanyua kichwa na Kusema *Sami Allahu Liman Hamida!*, na akabakia kasimama kwa mda wa kama ilivyokua Rukuu yake**. **Na kisha Akasujudu na Kusema *Subhanah Rabbi Al Aala*na akasjudu kwa kutumia mda kama ule alioutumia katika Kisimamo chake.'***(Sahih Muslim)*

Imam An Nawawi anasema kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hii ni Hadith yenye uthibitisho wa kuruhusika Kuirefusha Itidal**. **Na Imam Ibn Mulaqqin Al Shafii anasema kuhusiana na Hadith kama hii lakini imemalizia kwa kusema kua:** '**Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka kutoka kwenye Sijda na kukaa hadi nikadhania kua amesahau kusujudu tena**'*(Sharh Sahih Muslim)*

Na Imam Ibn Mulaqqin Al Shafii anasema kuhusiana na Hadithi nyengine kama hii ambayoimemalizia na maneno yasemayo kua.: **'Na Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka kutoka kwenye Sijda na kukaa hadi nikadhania kua ameshau kuhusiana na kusujudu tena'***(Sahih Bukhari na Muslim)*

Hivyo Imam Sirāj Al Dīn Abū Ḥafṣ ʿUmar b. ʿAlī b. Aḥmad Al Shāfiʿī Al Miṣr Ibn Mulaqqin anasema kua: '**Hadith hii inathibitisha Inaruhusika kukaa Itidal kwa mda mrefu na pia inaruhusika kukaa baina ya Sijda mbili kwa mda mrefu, hivyo haina hajakuachana na Mtizamo huu na kufuata Mtizamo wa Wanaosema kua Itidal na Jalasa Ni Nguzo ndogo za Sala'**

Naam...tukakumbushana haya kwa sababu kujaribu kuboresha Sala zetu kwani Ingawa Tunasali kila siku lakini Sala zetu si Kamilifu, zina kasoro nyingi sana.

Kwani anasema Imam Al Samarqandi kua amesema *Rasul Allahu Alayhi wa Salam* kua:**Mbinguni Kuna Malaika ambao tangu Kuumbwa kwao basi wao kazi yao ni Kumsujudia *Allah Subhanah wa Ta'ala*,wakiwa wamejawa na Khofu na Kuhshuu na wataendelea hivyo hadi siku ya Kiama. Na itakapofika siku ya Kiama Basi Malaika hao watasema**

سبحانك ما عبدناك حق عبادتك

Subhaanaka MaaAbdanaka Haqqa Ibadaatika.

*Tafsir:**Ya Allah Hakika sisi hatujakusujudia kwa haki kama inavyostahiki'***

Hivyo Kama ikiwa Malaika hao wameumbaa kwa ajili hio Watasema hivyo..Jee mimi nawe hali yetu ikoje?

Naam..tumeona kuhusiana na Jalasa kua kuna Mitizamo Tofauti, Juu yake na tumeona kua kuna aina tofauti za Jalasa.

Kwani kukaa katika Mkao wa *Iftirash* baina ya Sijda mbili na baina ya *Allahu Akbar* mbili hadi Mifupa yako ikatulia sawia hua ni Sunna kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Na ingawa hua inapendekezwa zaid kukaa mkao wa Iftirash lakini hata hivyo pia hua inaruhuska kukakaa mkao wa Iq'a ni mkao ambao Mtu anakalia Visigino huku vidole vya miguu yake vikiwa chini na vimeelekea Kibla.

Na pia kuna Mkao wa Tawwaruk ambao hua ni Kukalia Kalio la Kushoto huku Mguu wa Kushoto kusogezwachini ya mguu wa Kulia ambao unyayo wake hua ni wenye kusimama na vidole kuelekea Kibla, na Ingawa Wanazuoni wametofautiana kwa kuchagua Mkao Bora zaidi Miongoni mwa Mikao hii, lakini hata hivyo ubora wa mmoja kati ya aina hizi za mikao katika Sala hua ni kwa upande wa Sala ya Mwanamme tu.

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Jalasa(Kikao baina ya Sijda Mbili na Qaida yaani kikao cha Attahiyat zote mbili basi kwa upande wa Mwanamke yeye hua hana maamuzi ya Kuchagua Moja kati ya Mikao hii kwani Mwanamke katika Jalasa na Qaida zote za Sala hua ni mwenye kutakiwa kutumia Mkao wa Tawarruk tu basi.

Ambao kwa Upande wake hua ni Kalio la Kushoto Kukalia Ardhi huku miguu yake ikiwa imelekea katika Upande wa Kulia.

Na bila ya shaka haina haja ya kurudia sababu ya Wanawake kuruhusiwa mkao wa Tawarruk tu, kwani ni kutokana na uzuri wa Maumbile yake, ambao unampelekea kua ni lazima atumie Mkao huo tu ambao ndio unaomuainishia Unyenyekevu wake Ndani ya Sala Yake Mbele ya Mola wake.

Kwani amesema Imam Sufyan Ath Thawry kua amesema Mansur Ibn Ibrahim kua: '**Mwanamke hua ni mwenye kukaa upande kwenye Sala yake.'**

Na amesema Imam Nafii kua: '***Ummu ul Muuminin* Safiyat *Radhi AllahuAnha* alikua ni mwenye Kukalia chini katika Sala zake.'**

Hivyo hili liko wazi kwani Fikiria tofauti anayokua nayo Mwanammke katika Muonekano wa Maumbile yake, pale anapochuchumaa, au anapokaa kwa kuweka Makalio yake juu ya Visigino vyake juu, au anapoweka kwa kukalia Unyao wake**.**

Kwani hali hua ki Tofauti kabisa na pale anapokua amekaa mkao alioruhusiwa kukaa wa Tawarruk.

Naanasema Imam Muhammad Al Zuhayli kua: '**Miongoni mwa Masharti ya Kukubalika kwa Jalasa baina ya Sijda mbili ni kua:Kukaa Itidal (Kwa Utulivu) na kunyoosha Mgongo Sawia katika kukaa kwako, na hivyo hua haiyoshelezi kwa mtu kunyanyua Kichwa tu, au kukaa kwa kuupinda Mgongo katika Jalasa isipokua pale itakapokua kuna dharurah inayokubalika Kisharia.'***(Al Mutammad fi Fiqh Al Shafii)*

Kwani kwa maana hio basi tunapozungumzia kuhusiana na Jalasa au Ukaaji baina ya Sijda Mbili tunaona kua ingawa Kuna Masharti yake, na Sunna zake kulingana na Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini hata hivyo kama ikitokea kwa Mtu mwenye kusali akawa ni mwenye kua na Dharurah ya Kiafya labda tuseme basi hua inakubalika kubadilisha Mkao wa Jalasa.

Labda tuseme Mwanamke kutokana na kua maumvi ya Miguu au magoti n.k na hivyo hawezi kukaa mkao wa Tawarruk ambao ni lazima kwao wao kukaa basi anaweza kukaa mkao kama wa Mwanamme. Au labda Mwanamme hawezi kukaa mkao wa Iftirash, ambao ni mkao wa kukalia sehenu ya Unyauo wa Mguu wa kushoto na unyayo wa Kulia kusimamishwa na vidole vikielekea Kibla ambao ni Mkao wa Madhhab ya Hanafi, Al Shafii na Hanbal.

Au hawezi kukaa mkao huo na anaweza mkao wa Iq'a wa kukalia Visigino ambao ni mkao unakubalika zaid na Wanazuoni wa Hadith akiwemo Imam Al Bayhaqi, Imam Ibn Salah, Imam An Nawawi,Qadhi Al Iyadh na Mashaykh wa Kisalafi.

Na kama hawezi mkao huo basi anaweza kukaa mkao wa Tawarruk ambao ni wa Kukaa chini kalio la Kushoto huku mguu wa kushoto ukielea pembeni ya Mguu wa Kulia na Mguu wa Kulia ukiwa umesimamisha Nyayo.

Na kama hawezi hivyo basi anaweza Kukaa kulingana na atakavyoweza kulingana na hali ya afya yake. Yaani Mtu anatakiwa aoneshe tofauti ya baina Sijda ya kwanza na Sijda ya Pili,na ndio maana hiki Kitendo cha Jalasa kikawa inaitwa Ni Nguzo ndogo miongonii mwa nguzo za Sala.Kwa hivyo anatakiwa akae katika mkao ambao hata kama utakua unakirihishaNa hii ni kwa sababu, miongoni mwa Kanuni za Fiqh zinasema kua:

الكَرَاهَة تَزُولُ بالحَاجَة

‘Karaha hua inabatilishika kutokana na kuwepo kwa Haja’

Hivyo basi kila mmoja anatakiwa kutekeleza Jalasa kulingana na Uwezo wake kutokana na Afya ya Mwili wake, yaani usije ukamuona Mwanamme amekaaa Mkao wa Kike katika Sala, kisha ukamlaumu au ukamfikiria vibaya kwani inawezekana ikawa ana matatizo katika Vidole vyake vya Miguu, na hivyo hawezi kukaa mikao ya Kiume, ila kutokana na Dharurah aliyokua nayo basi kwa inaruhusika.

wani Ingawa inakubalika kwa mtu mwenye Dharurah kukaa kitako baina ya Sijda Mbili kwa kadri ya Namna atakavyoweza, ambapo kwa Upande wa Imam Abu Hanifa basi yeye anasema kua: ‘**Inapokua Mtu anadharura isiyomuwezesha kukaa kitako baina ya Sijida mbili basi hata Kuinua kichwa chake tu kutoka kwenye Sijida akatulia kidogo basi itatosheleza.’**

Na ingawa huo ni Mtizamo wa Imam Abu Hanifa lakini kuhusiana na Wanazuoni wengineo basi wametofautiana kuhusiana na Mtizamo juu ya Jambo hili kwani kuna Wanaosema kua kufanya hivyo hua si sawa na Kukaa, na hivyo hakuwezi kuhesabika kua ni sawa na Kitendo cha Jalasa kwa sababu hua kunafanana na kukaribiana na kitendo cha Sujud.

Kwani kuna Wasemao pia kua hata kwa Mtu anaepiga Magoti, kutokana matatizo ya miguu basi hua hatakiwa katika kupiga kwake magoti baada ya kutoka kwenye Sujud kabla ya kuingia kwenye Sujud ya Pili hatakiwi awe ameelemea mbele zaidi, kwani kuelemea mbele zaidi hua hakuwezi kuhesabika kua ni sawa na Kukaa sawasawaka katika Jalasa.

Na hivyo basi akielemea mbele zaidi basi atakua ni mwenye kubatilisha Sala yake. Lakini kama mtu husika atakua ni katika hali ya kusimamisha Sawia Mgongo wake bila kuelemea mbele zaidi katika kupiga magoti kwake baina ya Sijda Mbili kutokana na Udhuru Matatizo yake , basi hua inakubalika na hii ni kwa sababu ya kutokana na Kuusimamisha Sawia Mgongo wake hadai ukawa sawia na Mgongo Wa Mtu aliekaa au aliesimama.

Hivyo basi Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na Mkao wa Jalasa kulingana na Hali ya Mazingira ya Afya ya Mtu, kwani Kinachoangaliwa zaidi ni Jitihada za Anaesali katika Kusimamia Utekelezaji wa Kila hatua ya Sala kulingana Na uwezo wa Mtu husika. Kwa maana hio hua ni bora kwa mtu mwenye Udhuru kutekeleza Ibada ya Sala kulingana na uwezo wa hali ya Urahisi kwake. Na hivyo ajitahidi kujaribu kutofautisha hatua hizo za ndani ya Sala ili zisifanane, yaani isiwe kua Mtu amesujudu Sijda ya kwanza na kisha akanyanyua kichwa kidogo,au akajinyanyua na kushika Magoti na kuinama sana kama yuko katika hali ya mtu anasali huku akiwa kwenye kiti kutokana na Udhuru kisha akasujudu tena Sijda ya pili na ikawa haijulikani ni ipi sijda ya kwanza na ipi ni ya pili kwani zote zimechanganyika Na huenda zikahesabika tatu kwa sababu ya kua Jalasa yake imefanana na Sijda ya Mtu anaesali kwenye Kiti na hivyo Sala ikabatilika.

Ila ikiwa hakuna Njia nyengine kwake yeye mtu huyo mbali ya kujaribu kwake basi hapo hua hakuna tatizokwa sababu anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua:

﴿ فَاتَّقُوا اللَّهَ مَا اسْتَطَعْتُمْ وَاسْمَعُوا وَأَطِيعُوا﴾

Faattaqu Allaha maa AstataaAtum wasmaAau wa aAtiiau*(Surat At Taghabun 64:16)*

Tafsir: ***Hivyo Mcheni Allah Kwa Kadiri Mtakavyoweza Msikikizeni Na Mtiini.***

Ambapo maneno haya yanatudhihirishia kua Ni Wajibu wetu Kutekeleza Majukumu yetu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kadiri mtu atakavyoweza, na hivyo yale asiyoyaweza basi haina tutasamehewa.

Na Aya inatuhimiza pia kua kuna Umuhimu wa Kusikiliza Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Taala* ambayo ni Mepesi na kufuata Hukmu na Sharia zake na kuzikubali na Kuzitii. Kwani Sala ni Ibada Iliyowepesishwa na Miongoni mwa Kanuni za Fiqh Basi ipo ile isemayo:

الميْسُورُ لَا يَسْقُطُ بِالمِعْسُوْرُ

‘Amrisho lililo jepesi halibatilishiki kwa Jambo lililogumu’

Na tunapozungumzia kuhusiana na hii mada yetu na kisha kuiangalia kulingana na Maneno ya aya hii pia basi inatuonesha kua Tunatakiwa Tujitahid Kusali kwa Kadri itakavyowezekana kulingana na Afya zetu,kama Jalasa huiwezi Piga Magoti n.k, lakini tusiachane nayo Sala hata mtu ukiwa na dharura gani. Kwani ni bora kusali kuliko kutosali kabisa, kwa sababu kutosali kunamaanisha kupingana na kila neno la Aya hii na nyenginezo nyingi sana.

Kwani amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaponyayua Kichwa chake kutoka kwenye Sujud basi hasujudu hadi awe ni mwenye kusimama sawasawa,na anaposujudu hunyanyua Kichwa chake na Hasujudu tena hadi atakapokaa na kunyooka mgongo,na alikua akiusogeza mbele mguu wake wa kushoto'** (*Sunan Ibn Majah)*

Na amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alisema kuniambia mimi kua:**

إذا رفعت رأسك من السجود فلا تقع كما يقعي الكلب

Unaponyanyua Kichwa chako kutoka kwenye Sujud Usichutame kama anavyoka Mbwa. Bali weka Makalio yako juu ya baina ya Miguu yako na ruhusu vidole vyako Vigusane na ardhi'*(Sahih Ibn Majah)*

Naam..tumeanza na Hadith mbili tofauti zenye kuelezea hali ya Jalasa na katazo la mkao wa Kuchutama kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Ambapo tunapoiangalia kuhusiana na Hadith ya pili ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* yenye katazo na amrisho ndani yake basi tunaona kua Wanazuoni wametofautiana juu ya kilichokatzwa ndani yake.

Kwani kuna walioifaham kua inamaanisha katazo la Kusimamisha Nyayo na kisha kukalia Visigino. Na kuna wanaosema kuakulichotakazwa ni mkao wa Kukalia Makalio huku Magoti yakiwa yamesimama, ambako kunafanana na mkao wa kuchutama kwa Mbwa.

Hivyo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: **Ama kuhusiana na Kukalia Visigino, basi tumetaja Hadith zilizokataza na mbali ya kua ziko nyingi lakini hakuna iliyothibitishwa Usahih wake.Na kuhusiana na kukalia visigino basi kumethibitishwa na Nukuu ya Tawus ambae amesema kua: Sisi tulimwambia Ibn Abbas kuhusiana na Kukalia Visigino ambapo nae akasema: Hio ni Sunna ya R*asul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam.***

Hivyo nasi tukasema: Lakini mbona sisi tunaona kua kukaa hivyo mbele za watu hua ni ufidhuli?. Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anh*u akasema: La Kukaa hivyo hua ni Sunna ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam**(Sahih Muslim)***

Ama katika Sunan Al Bayhaqi basi Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: Miongoni mwa Sunna za mikao ya ndani ya Sala basi Makalio yako yaguse visigino vyako baina ya Sijda Mbili.

Imam Al Bayhaqi ameitaja hii Hadith ya Ibn Abbas na kisha akaitaja Hadith ya Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum* ambae yeye baada ya kutoka kwenyw Sijda ya Kwanza basi hua ni mwenye kukalia visigino na kukandamiza ncha za Vidole vyake,na alikua akisema Ni Miongoni mwa Sunnah.

Kisha Imam Al Bayhaqi akamnukuu Tawus aliekua akikaa hivyo, baada ya kuwaona Masahaba wakikaa hivyo Abd Allah Ibn Umar, Abd Allah Ibn Abbas na Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhum.*

Imam Al Bayhaqi anasema kua Ukaaji huu hua unatosheleza kulingana na Sunna kama tulivyonukuu kutoka kwa Ibn Abbas na Ibn Umar kua:Walikua wanaweka Vidole vyao Ardhini na Makalio yao juu ya Visigino vyao, na Magoti yao juu ya Ardhi.Kisha Imam Al Bayhaqi akanukuu Hadith zote zinazokataza kukaa hivyo na na Sanad zake na kuzikosoa zote na kufafanua udhaifu wake zote.

Na kisha akasema kua Hadith ya Ibn Abbas na Ibn Umar kua ni Sahih.Kisha Imam Al Bayhaqi akanukuu hadith ya Abu Ubaid kutoka kwa Shaykh wake Abu Ubaidah amnae amesema kua: I'qa hua ni Kukandamiza Vidole ardhini na Kukalia Visigino na kuweka Magoti Ardhini.

Na kuchutama hua ni Kuweka Makalio chini na kusimamisha Magoti kama anavyokaa Mbwa au Simba: Hivyo mkao huu hua ni tofauti na mkao waliouelezea Ibn Abbas na Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*. Kwani Mkao huu wa Kama akaavyo Mbwa ndio Uliokatazwa. Na tuliyoyanukuu kutoka kwa Ibn Abbas na Ibn Umar ni Miongoni mwa Sunna.'

Kwani Imam An Nawawi anaendelea kusema kua Imam Al Bayhaqi anaendelea kusema kua; Ama kuhusiana na Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* isemayo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitukataza sisi Kumfuata Shaytan.

Basi inawezekana kua Maneno haya yanazungumzia kuhusiana na Mkao wa Attahiyat ya Mwisho, hivyo maneno haya hayapingani na Kauli za Ibn Abbas Na Ibn Umar kuhusiana na Kikao cha baina ya Sijda mbili.

Na haya ndio maneno ya mwisho ya Bayhaqi *Allah Rahimahumu Allah*, kwani alikua Mtaalamu Mahiri na mwenye kunufaisha sana na huelezea vya kutosha na mwenye kuandika kwa kina*(Al Majmuu Imam An Nawawi)*

9-TMAI'NINAH KUTULIA BAINA YA SIJDA MBILI

Naam kama tulivyoona hapo kabla katika Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* iliyosema kua: **'Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaponyayua Kichwa chake kutoka kwenye Sujud basi hasujudu hadi awe ni mwenye kukaa sawia**' *(Sunan Ibn Majah)*

Na pia katika Hadith ya Rifaa Ibn Rafi *Radhi Allahu Anhu* ya Bedui alierudishwa mara 3 kusali na *Rasul Allah Salallahu Allahu Alayhi wa Salam* kutokana na kukosekana kwa Utulivu ndani ya Sala yake, na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamfundisha kwa kumsisitizia Umuhimu wa Kua na Utulivu katika Kila Hatua.

Kwani hata katika Kukaa Kitako baina ya Sijda Mbili katika Mmoja kati ya Mikao ya Miguu iliyoruhusika kama tulivyoelezea katika Jalasa, basi katika Kukaa kwake Mtu anatakiwa sehemu ya Mbele ya Mikono yake yaani kuanzia Kwenye Kisugudi hadi kwenye Viganja iwe imekaa sambamba kwa kunyanyuka juu kidogo ya Mapaja yake.

Huku Kiganja chake cha mkono wa Kulia kikiwa juu ya Paja la Mguu wa Kulia karibu na Goti la Mguu wa Kulia au kwenye Goti kabisa.Na kwa upande wa Mkono wa Kushoto na Paja la kushoto basi hali inayakiaa iwe hivyo hivyo.

Na juu ya Hili kuna Makubaliano ya Wanazuoni kama alivyosema Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki, Imam Al Juzayy na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi pia. Na baada ya kukaa katika Hali hio basi Mtu anatakiwa Kutulia ndani yake.

Kama alivyosema Imam Taqi Ad Din Abu Al Fat-h Muhammad Ibn Ali In Wahb Ibn Muti Ibn Abi Ataa Ibn Daqiq Al Idd Al Shafii kua: '**Kukaa na Kutulia kwa Utulivu baina ya Sijda Mbili kumetajwa**

mara kwa mara na Wanazuoni wa Fiqh kua ni Fardhi wa yale yaliyotajwa Katika Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'*(Ahkam Al Ahkami)*

Ambavyo ndivyo alivyosema Shaykh Uslami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi pia kua: '**Kukaa Kitako baina ya Sijda Mbili hua ni Wajib na Kutulia ndani yake pia hua ni Wajib, ambako hakutakiwi kuwe ni kwenye kuchukua Mda mrefu.'**

Ambapo kulingana na mtizamo wa Imam Al Ramli basi ni kua hua haipendekezwi kukirefusha kikao cha baina ya Sijda mbili ingawa kufanya hivyo hua hakubatilishi Sala. Ambapo kwa mtizamo wa Imam Ibn Hajar Al Asqalani basi nikua Sala hubatilika kama urefu wa kikao hicho utakua ni wenye kuzidi dhikr stahiki'*(Fatawa An Nawawi)*

Na kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni basi katika Kukaa kwake Mtu ndani ya Kikao hicho anatakiwa Atulie angalau kwa mda wa kusema *Subhanah Allah.*

Kama anavyosema Imam Ibn Aabidin Ash Shami Al Hanafi kua: '**Hua ni Wajib kukaa kwa Utulivu Baina ya Sijda mbili kwa urefu wa mda wa kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema Subhanah Allah**'*(Radd Al Mukhtar)*

Na kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi tunaona pia kua: '**Ingawa kukosa utulivu katika Kikao cha Baina ya Sijda mbili hakubatilishi Sala, lakini hata hivyo Mtu anatakiwa kuleta Sijdat Sahw pale atakaposahau kutulia**. **Na atakapoacha kwa Makusudi basi hua ni mwenye Kufanya Dhambi ndani ya Sala, ambako kutampelekea Kuirudia Upya Sala yake hio yenye Kasoro ijapokua Sala hio haijabatilika.'** *(Nur Al Iddah)*

Hivyo Wanazuoni wanakubaliana kua Kukaa na Kutulia baina ya Sijda mbili kua ni Wajib kama ilivyotajaa katika Khashiyat Ibn Abidin ya Imam Ibn Abidiin Al Shami, Mawahib Al Jalil ya Imam Muhammad Ibn Muhammad Al Khattab, Al Majmuu ya Imam An Nawawi, Al Mughni ya Imam Ibn Qudamah.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Al Allamah Al Qadhi Al Imam Mustafa Ibn Saad Ibn Abduh Al Suyuti Al Ruhaybani Ad Dimashq Al Hanbali katika *Matalib Uli Nuha* kua:**'Kukaa kitako na Kutulia baina ya Sijda Mbili ni moja Kati ya Nguzo za Sala ambayo haiwezi kuachwa kwa lolote lile**. **Kwani imeitwa Nguzo kwa sababu Sala haiwezi kukamilika bila ya kutekelezwa kwake, na ndio maana ikafananishwa na nguzo zinazoisimamisha Nyumba, na baadhi wamsema kua ni Fardhi**'*(Matalib Uli Nuha)*

Kisha Imam Mustafa Al Suyuti akasema kua '**Sala ina Nguzo 14 na Nguzo ya 8 ni Kuinuka Kutoka katika Kusujudu na Nguzo ya 9 ni Kutulia baina ya Sijda mbili**. **Na hii ni kwa Sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwambia yule Mtu aliekosea Kusali kua:*Thuma Irfaa hata Taatadil Jalisan* - Kisha Nyanyuka Utulie hadi Upate Utulivu katika kukaa kwako**, **Hivyo utulivu baina ya Sijda mbili unatakiwa kupatikana japo hata kaa mda kidogo.'**

Na anasema Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Manufi Al Misri Al Ansari Shams Ad Din Al Ramli Al Shafii kua: '**Kukaa na kuupata Utulivu baina ya Sijda Mbili za Sala hua ni Moja kati ya Nguzo za Sala**. **Iwe Sala ya Fardhi Ama ya Sunnah, na hivyo kama ikiwa Mtu atakaa kitako na kisha akatikisika kaa kuogopa kitu labda basi hio hua haitoshelezi hivyo hua ni lazima arudi kwenye utulivu kisha ndio aingie kwenye Sidja ya pili Na asipofanya hivyo kwa Makusudi basi Sala yake hua ni Batili.'**

Imam Al Ramli anaendelea kusema kua: **'Imepokewa kutoka kwa Imam Al Shafii kua alikua akikaa kwenye Visigino vyake, huku Vidole vyake vikiwa vimekandamizika Ardhini na Magoti yake yakiwa Ardhini.Na Kila mkono wake ukiwa juu karibu na kila Goti la Mguu wake, huku vidole vikiwa vimepinda kama kulikamata Goti.**

Na kukaa hivyo hua haidhuru kwa sababu ni miongoni mwa Sunnah, na hikma ya kulishika Goti katika kukaa huko hua ni kuvizuia vidole kutokana na kucheza cheza,na hivyo mkao huu hua ni wenye kumkaribisha zaidi Mtu katika kumuingiza kwenye Khushuu.

Na imenukuliwa pia kutoka kwa Imam Al Shafii alikua akivibana na kuvielekeza vidole katika Upande wa Kibla kama ifanywavyo kwenye Sujud.'*(Nihayat Al Muhtaj Ila Sharh Al Minhaj)*

ADHKAR BAINA SIJDA MBILI

❖❖❖

Kwani mara baada ya kupatikana kwa Utulivu katika Kikao cha bain ya Sijda mbili basi kitu kinachofuatia hua ni kama inavyoelezea Hadith ifuatayo ya Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* isemayo:

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ: كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ بَيْنَ السَّجْدَتَيْنِ: «اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَاهْدِنِي وَعَافِنِي وَارْزُقْنِي»

Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema baina ya Sijda zake mbili maneno yafuatayo:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَاهْدِنِي وَأَجِرْنِي وَارْزُقْنِي وَارْفَعْنِي

Allahumma ighfir li wa'rhamni wa'jburni wa'hdini wa'rzuqni

Tafsir: **Ewe Mola wangu, Niingize kwenye Rehma zako, Na Uniongoze, Na unipe Nguvu na uwezo, Na Uniruzuku.'** *(Sunan Abu Daud, Imam At Tirmidhi)*

Naam..kabla ya kuendelea zaidi basi kwanza tukumbushane kua tunapoangalia maneno ya Dua hii basi hua tunaona Umuhimu wake na uzito wake katika Maisha ya Kila mmoja weru na Hivyo Kila mmoja wetu kwani ndani yake Dua hii katika maneno ya mwanzoni kabisa tunaona kua kuna neno **Allahuma ighfirli** lenye kuonesha kuomba Msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta'al*a na kuthibitisha nia ya Kutaka Kujitakasa kutokana na Kasoro za Kiumbe mbele ya Mola wake.

Kisha maneno yanayofuatia ni **Warhamni** yenye kuthibitisha Umasikini wa Kutokua na uwezo juu ya kitu chochote bila kuwepo Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kuomba Muendelezo wa Rehma hizo hapa Duniani na Akhera.

Kisha kinachofuatia ni **Wahdini** yaani Kuomba Muongozo ambao ni wenye kuhitajika kwa Kila Ibn Adam ili apate kuongoka kwa Kufuata njia Sahih kama aliyoiamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kisha kuna neno **Wajburni** lenye kuonesha kuomba kwa Unyenyekevu kutokana na Kujua kua Ibn Adam Hana Uwezo wowote wa Kiafya wala Kiakili kwa ajili ya kutekeleza Majukumu yake mbele ya Mola wake bila ya kupewa uwezo huo na Mola wake.

Kisha kuna neno **Warzuqni** lenye kuthibitisha kua Mbali ya Ujanja wake wote lakini bado Ibn Adam ni mwenye kumtegemea *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kila kitu kinachohusiana na Riziki yake.

Na kisha kuna neno **Warfa-Aani** ambalo ni lenye kuonesha maombi ya kutaka kunyanyuliwa Darja kutokana na Ibada na Ukaribu wa anaeomba kwa Mola wake.

Na hivyo Maombi haya hua ni yenye kuonesha kua Muombaji ni mwenye kutegemea Kukubaliwa Ibada yake na Kupandishwa Darja hapa Duniani na Akhera pia.

Na tunapoangalia Hadith ya Hudhaifah Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* inayozungumzia kuhusiana na Sala ya *Rasul Allah Salallauu Alayhi wa Salam* basi tunaona kua anasema Hudaifah *Radhi Allahu Anhu kua:*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema katika Sala yake katika wakati wa baina ya Sijda mbili maneno yafuatayo:**

رب اغفرلي، رب اغفرلي

Rabbi ighfirly, Rabbi Ighfirly - Ewe Mola wangu Nisamehe, Ewe Mola wangu nisamehe*(Sunan Ibn Majah, Sunan An Nasai)*

Naam..hivyo basi kuomba Dua baina ya Sijda mbili hua ni Suna Iliyotoliliaa mkazo. Na ingawa hata hivyo kutosema kitu baina yake hua hakubatilishi Sala ya Mtu Husika, ila ni bora zaidi kwa wale wasiojua basi wawe ni wenye kusema *Rabbi Ighfirly.*

Kwani imeelezewa katika *Mawsuah Al Fiqhiyah* kuhusiana na Dua katika baina ya Sijda mbili kua: **'Katika Wakati wa Kukaa baina ya Sijda Mbili hua inapendekezwa Kuomba Msamaha kwa *Allah Aubhanah wa Ta'ala.***

Na hii ni kulingana na Mtizamo wa Madhhab yote Hanafi,Maliki, Shafi na Hanbal na hii ni Kutokana na Uthibitisho wa Hadith ya Hudhayfah Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* alipokua akisali na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua baina ya Sijda Mbili alikua akisema *Rabbi Ighfirly Rabbi Ighfirly.*

Na hata hivyo kuomba Maghfira hua si Wajib na hii ni kwa sababu*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumwambia Yule Bedui aliekua hajui Kusalikua afanye hivyo baina ya Sijda mbili. Ambapo kwa upande wa Imam Ahmad Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh na Imam Abu Daud basi wao wamesema kua Kuomba Maghfira baina ya Sijda mbili hua ni Wajib.' *(Al Mawsuah Fiqhiyyah)*

Na Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na Idadi yake Istighfarhio baina ya Sijd Mbili kua isipungue mara Tatu kama vile ambavyo ilivyo kawaida kwa Dhikr zote nyenginezo za ndani ya Sala kua hazitakiwi kupungua chini ya Mara tatu, ingaaa inaweza kuongeza idadi ambayo ni vizurikua katika hali ya Witr kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapenda Idadi ya Witr.

Ambapo anasema Imam Muhammad Al Shanqiti kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alikua akiomba Maghfira, na uwezo wa Kutekeleza majukumu yake mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* baina ya Sijda mbili, kwa sababu hio ni sehemu ya kuomba Dua.**

Ingawa Kuna Mitizamo miwili juu ya Jambo hili kutoka kwa Wanazuoni, kwani kuna wasemao kua hii hua ni sehemu ya Kuomba Dua hivyo Mtu anaweza kuomba Dua aitakayo.

Na wengine wanasema kua katika sehemu hii Mtu anatakiaa asome kile ambacho amekisoma *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na mtizamo huu una nguvu zaidi, lakini kama ikisa mtu hakuhifadhi Dua hio basi anaweza kuomba Dua aitakayonaSababu inayoifanya kukubalika kwa dua yeyoteni kulingana na Mitizamo miwili ya Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ambapo Mtizamo wa kwanza ni Kuomba Dua na Mtizamo wa pili ni kusema Maneno Maalum,hivyo kama ikiwa hayajui maneno hayo maalum basi na aombe Dua, na Huu ndio Mtizamo wa Wengi Miongoni mwa Wanazuoni.

Hivyo kama Mtu hakuhifadhi maneno hayo basi na asome Dua yeyote aijuayo kwa ajili yake na wazee wake n.k na hakuna ubaya juu ya hiloLakini inapendekezwa zaidi kusoma Dua alizosoma *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'**(Sharh Az Zad)***

Anasema *Shaykh Ul Islami* Imam Abu Zakariyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Na baina ya Sijda mbili wakati Mtu anapokaa katika Sala basi anatakiwa asome Dua Ifuatayo: *Rabbi Ighfirli, Rabbi Ighfirli* na hii ni kutokana na Hadith ya Hudhayfah *Radhi Allahu Anhu*: Na pia kutoka katika Hadith ya Maimuna *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua amemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema katika Sala baina ya Sijda mbili maneno yafuatayo:Rabbi Ighfirli Wa Arhamni Wajburni Wa Arfaanu Warzuqni wahdini***(Sunan Al Bayhaqi)**

Hivyo ni vizuri kwa Mtu Kuomba kulingana na Sunna ili kuweza kua katika Upande SalamaNa hivyo ni bora kutumia moja kati ya Dua mbili hizi zilizotajwa katika Hadith hizi' *(Al Majmuu)*

Ambapo kwa Upande wa Al HafidhAl Imam Abd Rahman Ibm Ahmad Ibn Rajab Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Ama kuhusiana na Hukmu ya Dhikr baina ya Sijda mbili kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad. Ni kua hukmu yake ni sawa na Tasbih nyenginezo za kwenye Rukuu na Sujud, ambazo hua ni Wajib, hivyo Sala hubatilika pale zisiposomwa ndani yake inapokua ni kwa makusudi**. **Na kama ikiwa Mtu atakua hakufanya kwa Makusudi bali amesahau basi Mtu husika humbidi kutekeleza Sijdat Sahaw**. **Ambapo pia kwa upande mwengine basi Amesema Imam Ahmad pia kua hua si Wajib.'**

Ambapo kwa upande wa Al Alama Imam Ahmad Ibn Muhammad Ibn Harun Ibn Yazid Abu Bakr Al Khallal Al Bagdadi Al Hanbal basi yeye anasema kua: '**Kulingana na Mizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi ni kua hua inaruhusika kama mtu hakutamka kitu baina ya Sijda mbili na huu pia ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni.'***(Fat-h Al Barr li Ibn Rajab)*

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Abu Ikhlas Hasan Ibn Ali Ibn Shurunbulali Al Wafai Al Hanafi kua: '**Kwa upande wa Skuli ya Madhhab yetu basi hua hakuna Dua maalum ya kusoma baina ya Sijda mbili, lakini hata hivyo ni bora katika sehemu hii kufanya *Istigfar(Rabbi Ighfirlli)* ili kuepuka utofauti wa Mitizamo ya Wanazuoni.'***(Maraqi Al Falah)*

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Imam Ibn Abidin Al Shami na kwa upande wengine tunapowaangalia Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kuhusiana na Dua baina ya Sijda mbili basi ingawa wamesema kuna Imam Ibn Aabidin na Imam Al Shurunbulali kua: '**Hakuna Dua maalum katika kikao cha Baina ya Sijda mbili ila inapendekezwa kusema Rabbi Ighfirliili kuepuka Utofauti wa Mitizamo ya Wanazuoni.'**

Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wamesema hivi kaa sababu kulingana na Mtizamo wao katika Vithibitisho vya Hadith zilizotumika kuthibitisha Dua hizi baina ya Sijda mbilikua Hadith hizo zinazungumzia kuhusiana na Vitendo vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa SalaM* katika Sala zake za Sunna.

Ambapo kuhusiana na Sala za Fardhi basi ziko kama alivyozisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na namna alivyoamrishakua zisaliwe.

Kwa maana hio basi kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa tunaona kua Katika Sala za Fardhi hua hakuna ulazima wa Kutamka Dhikr au Dua hizi baina ya Sijda mbili.Lakini hata hivyo hua inapendekezwa zaid kusoma Dhikr hizo kama alivyosema Imam Ibn Aabidin Al Shami katika *Radd Al Mukhtar.*

Kwani baada ya kumuangalia Imam Ibn Aabidin Al Muhaqqiq wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi tunamkamataImam Al Muhaqqiqin wa Madhhab Ya Imam Al Shafii na Madhhab mengineyo ambae ni Imam Ibn Hajar Al Haythami Al Makki Al Shafii ambae anatuambia kua:**'Baina ya Sijda mbili hua Ni Sunna Kusema:**

قَائِلًا رَبِّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَاجْبُرْنِي وَارْفَعْنِي وَارْزُقْنِي وَاهْدِنِي وَعَافَنِي لِلِاتِّبَاعِ فِي الْكُلِّ وَسَنَدُهُ صَحِيحٌ زَادَ فِي الْإِحْيَاءِ وَاعْفُ عَنِّي

Rabbi Ighfirli Wa Arhamni Wajburni Wa Arfaanu Warzuqni Wahdini Waafini Na hii ni kwa Sababu ya kua Kufanya hivyo hua ni Kufuata Nyayo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kila neno Alilolisema kama ilivyosemwa kwa Hadith yenye Sanad Sahih.'

Imam Ibn Hajar Al Haytami anaendelea kusema kua: '**Ama kuhusiana na neno Wa Aaf aAni basi limeongezwa katika Ihya Ulim Ad Din na Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali'***(Tuhfah Al Muhtaj)*

Kwani Hujjat Ul Islami ameongezea neno Wa Aaf Aani kwa sababu hua inaruhusika kufanya Hivyo kama alivyosema Imam Shurunbulali, Imam Al Shawqani, Imam Ibn Aabidin na pia kama anavyosema Shaykh Ul Islami Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: '**Imam Al Mutawwali ambae ni Muandishi wa Al Tatimah amesema kua: 'Sio Dua hizi mbili tu ndio Maalum kusomwa baina ya Sijda Mbili bali Mtu anaweza kusoma Dua yeyote na kufanya hivyo Itakua ni Sunna, ila ni bora kusoma kama zilivyosema Hadith'***(Sharh Al Muhadhdhab)*

Na Hivyo wale wanaosema *Rabbi Ighfirli Wa Arhamni Wajburni Wa Arfaani Warzuqni Wahdini Waaf Aani.* Basi hii hua ni Kulingana na Mtizamo waHujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi, katika Ihya Ulum Ad Din na hakuna Ubaya ndani yake kuisoma kwa sababu maneno hayo *Waaf Aani* ni sehemu ya Dua ambayo yanamaanisha Na Unisamehe Dhambi zangu.

Ama kwa upande mwengine tunapoziangalia Hadith zinazozungumzia kuhusiana na Dua ya Baina ya Sijdambili basi tunaona kua '**Anasema Imam An Nawawi kua Hadith ya Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu iliyonukuliwa na Imam Abu Daud,Imam Al Tirmidhii, na wengineo basi ni Hadith yenye Mnyororo Sahih unaowashikamanisha Wanukuzi wake,Na Imam Al Hakim pia amenukuu katika Mustadrak Al Hakim yake huku akisema kua Isnad (Mnyororo wa muunganisho wa Walionukuu) yake ni Sahih.'**

Na maneno yaDua iliyomo kwenye hadith ya Imam Abu Daud ni:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَعَافِنِي وَاهْدِنِي وَارْزُقْنِي

Allahuma Ighfirly, Wa Arhamni, Waafini, Wahdini Warzuqni

Ambapo kwa upande wa Hadith ya Imam Al Tirmidhi ina maneno kama haya isipokua ndani yake kuna na neno Warfaa Ani

وَارْفَعْنِي

Ambapo katika Hadith ya Imam Ibn Majah haina neno Waarfaa Aani lakini ina neno

وَاهْدِنِي

Wahdini.

Na Hadith ya Imam Al Bayhaqi ina maneno yasemayo:

رب اغفر لي وارحمني واجبرني وارفعني وَاهْدِنِي

Rabbi Ighfirly, Wa Arhamni, Waafini, Wajburni, WarfaAani, Wahdini Warzuqni.

Hivyo hii inaonesha kua hakuna Dua Maalum ya Kusoma bali inawezekana kusomwa Dua yeyote.*(Al Majmuu)*

Hivyo tunaporudi kwa Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali na neno hili Waaf-Aani katika Dua ya Baina ya Sijda Mbili.Basi tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimfundisha Sahaba wake mmoja Dua yenye Maneno haya katika Hadith isemayo:

'Amesema Ibn Abi Aufa *Radhi Allahu Anhu* kua, kuna Mtu alikuja Kuonana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na akamuomba *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amfundishe Dhikr na Dua za Ndani ya Sala, Kwani Mtu huyo alikua hajui kusoma Qur'an. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Mtu huyo kua Asome Dua ifuatayo kwenye Sala zake:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَاهْدِنِي وَارْزُقْنِيوَعَافِنِيوَاعْفُ عَنِّي

Allahuma Ighfirli wa Arhamni, Wahdini, Warzuqni, WaAafini, Wa Aafu Aani.

Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Mtu huyu atakua amejaza Kheri kwenye Mikono yake kutokana na Dua hii'(*Imam Al Bayhaqi Sunan Al Kubra)*

Kwa maana hio basi Hujjat Ul Islami amechukua Dua hii na kupendekeza kua iwe ndio yenye kusomwa katika Sala baina ya Sijda Mbili. Na tukitaka kujua zaidi sababu nyengine kwanini Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali akaichagua Dua hii, basi inabidi turudi katika Ufafanuzi wa neno Waaf Aani kama alivyolofafanua Imam Al Ghazali Mwenyewe ambae anasema kuhusiana na neno Al Aafuwu ambalo ndio lililotoa neno Af Aani kua: '**Neno Al Aafuwu hua linamaanisha Kuondoa Dhambi na Kua Huru kabisa kutokana na Dhambi zote Ambapo neno Al Aafuwu hua linakaribiana kumaana na neno Ghafur lakini neno Aafuwu linazama zaidi kimaana kuliko Ghafur na hii ni kaa sababu nenl Ghafur hua ni lenye Kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kuyafunika tu na kutoyaangalia Madhambi, na wala si Kuyafuta.'***(*Maqasid Al Asna)*

Subhanah Allah! Yaani hapa ndio Tunaona Maana ya ile Dua ya Siku ya Laylat Al Qadr aliyoifundisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo: ***'Allahuma Innaka Aafuwun Tuhibu Al Afwa Fa Aaf Aani.'***

Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Munir Al Dimashqi basi yeye anasema kua: '***Al Aafuwu* ni Sifa ya Haki ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kuyafuta Madhambi yoote ya Mja katika vitabu vyote vya hesabu na hivyo Mtu husika hatohesabiwa kuhusiana na Madhambi hayo katika Siku ya Malipo, na pia Dhambi hizo hufutwa ndani ya Moyo wa Mtu husika na hivyo hatoona aibu juu ya Madhambi hayo kwani badala yake hua ni mwenye kuandikiwa wema.Na kwa Maana hio basi neno Al Aafuwun lina kina zaidi kimaana kuliko Al Ghafuru kwa sababu Al Ghafuru humaanisha Kuyafunika Madhambi na Al Aafuwu humaanisha Kuyafuta kabisa'***(*Al Nafahat Al Salafiyah)*

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Rajab Al Hanbal basi yeye anasema kua: 'Neno Al Ghafur halitekelezeki hadi pale adhabu itakapobatilishwa au kuondolewa na hii ni kwa sababu Al Ghafur hua ni ngao yenye kuondoa madhara na usamehevu hua ni wenye kupatikana baada ya kuwepo kwa adhabu, kwa maana hio basi mashakil yote ya kidunia hua ni yenye kutuondolea dhambi na hua yanajulikana pia kama adhabu, wakati Al Afuwu hua ni lenye kutekelezeka iwe kwa kuwepo kwa adhabu ama la'*(*Jamii Ulumu wa Al Hikam)*

Kwani hizo ndio Hikma za Hujjat Ul Islami Abu Hamid Muhammad Al Ghazali katika kuongeza *Wa Aaf Aani* ndani ya Dua ya baina ya Sijda Mbili.

Hivyo katika Kuangalia kwetu kuhusiana na Adhkar na Dua zinazosomwa katika Hatua ya Sala ya baina ya Sijda mbili, basi kama tulivyoona tunaona katika Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* inayoelezea kuhusiana na Yule Mtu aliesalikisha akarudishwa mara 3 na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kua akasali tena.

Na mwishowe Mtu huyo akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Amfahamishe Kusali kwani yeye amejitahid na hivyo alivyofanya basi ndio kwa uwezo wake wote.*Hivyo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamfahamisha hatua kwa hatua kama tulivyoona hapo kabla katika Kuielezea hadith hio.

Na*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipofikia katika kuelezea hatua ya Kusujudu Sijda mbili ndani ya Sala basi alisema:

ثم اسجد حتى تطمىءن ساجدا ثم ارفع حتى تسثوي وتطمىءن جالسا ثم اسجد حتى تطمىءن ساجد

Kisha Sujudu hadi Ujisikie Umetulia kwenye Sijda yako, na Kisha Nyanyuka Ukae kitako hadi ujisikie kua Umetulia katika Kukaa kwako, na Kisha Sujudu Tena hadi ujisikie kua Umetulia ndani ya Sijda yako.

Ambapo hii ni Hadith ambayo ina makubaliano ya Ijmaa ya Wanazuoni Juu yake kuhusiana na Usahih wake na kuhusiana na Vitendo na Hatua za Sala zilizoelewa Ndani yake na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Na ndio maana mara kadhaa imekua tunairudia rudia katika kuchomoa Vithibitisho na kuvionesha kulingana na Mitizamo ya Masahaba na Wanazuoni *Radhi Allahu Anhum.*

Na tunapoangalia kuhusiana na Amrisho la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Sijda mbili na kikao kilichopo baina yake basi tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha kuhusiana na Kikao hiki kua kisiwe ni cha Mda mrefu bali kiwe ni cha Kumthibitishia Mtu anaesali kua Ametulia ndani yake kikao hiki.

Na kama tulivyoona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuamrisha Kuhusiana na ni nini cha Kukisoma ndani yake baina ya Sijda Mbili na mara ngapi.Ila kulingana na Hadith nyenginezo basi Imethibitishwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisema manemo ya Dua ndani yake kama:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَعَافِنِي وَاهْدِنِي وَارْزُقْنِي

Na ndio maana baadhi ya Wanazuoni wakasema kua Si Wajib kufanya Dhikr ndani yake Kikao hiki bali ni Sunna.Na pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akirukuu akinyanyuka Kutoka kwenye Rukuu na Kusujud na Kukaa baina ya Sijda Mbili, kwa kutumia Mda unaofanana katika Kila Rakaa.Yaani kama atatimia Sekunde 10 katika Rukuu basi na Katika Sujud Atatumia Sekunde 10 katika Rakaa zote za Sala husika.

Na kama atatumia sekunde 6 kwenye Itidal yaani kisimamo cha kutoka kwenye Rukuu basi na kwenye Jalasa baina ya Sijda mbili atatumia sekunde 6 pia. n.k

Ambapo hata hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua Akitumia Urefu wa Mda tofauti katika Sala zake.Yaani alipokua akisali peke yake basi alikua akitumia mda mrefu zaidi katika Kila hatua ya Sala yake kwa kusoma Aya nyingi zaidi za Qur'an katika Visimamo, Dhikr nyingi zaidi katika Rukuu na Sujud, Dua Nyingi zaidi katika Itidal na Jalasa na Attahiyat n.k.

Ambapo hali hii ilikua tofauti na anapokua anasalisha Msikitini katika Sala za Jamaa ambapo alikua akitumia Mda mdogo katika Sala zake hizo kwa sababu ya kutotaka kuwafanyia Ugumu wale Wanaomfuata Nyuma yake.Kwani anasema Al Faqih Al Hafidh Imam Abu Hasan Ali Ibn Khalaf Ibn Abd Al Maliki Al Battal Al Bakri Al Qurtubi Al Maliki kua:

‘Urefu wa Rukuu na Sujud za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ulikua ukitofautiana, kulingana na namna anavyosali baina ya anapokua peke yake na anapokua katika Jamaa. **Kwani katika Sala za Jamaa basi Rukuu zake na Sujud zake hazikua Ndefu sana**. **Lakini alipokua akisali peke yake basi alikua akirefusha Rukuu zake na Sujud zake kwa kurudia rudia sana visomo**

vilivyomo ndani yake. **Na hakuna Ushahidi kua alikua ni mwenye kurefusha Sijda ya Rakaa yake ya Mwisho'***(Sharh Sahih Bukhari Imam Ibn Battal)*

Kwani hii ni hali tofauti na Wanavyofanya wengi miongoni mwa Maimam wetu leo hii katika Kusalisha Sala zao, kwani wengi hua Wanapenda Visomo virefu wanapokua Wanasalisha bila kujali wala kufikiria kuhusiana na Maamuma kua miongoni mwao kuna Wagonjwa, Wazee, n.kWanasahau kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua kweli akisoma Sura ndefu lakini pale anapokua peke yake.

Hivyo labda tuwakumbushe kwa kuangalia kuhusiana na kisa cha yule Sahab ambae alikua akipendwa sana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aitwae Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* ambae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwambia wazi wazi kua: **'Hakika Mimi nakupenda Ewe Muadh!'**

Na Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* alikua ni Imam wa Watu wake.

أَخْبَرَنَا قُتَيْبَةُ، قَالَ حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ، عَنْ جَابِرٍ، قَالَ صَلَّى مُعَاذُ بْنُ جَبَلٍ لأَصْحَابِهِ الْعِشَاءَ فَطَوَّلَ عَلَيْهِمْ فَانْصَرَفَ رَجُلٌ مِنَّا فَأُخْبِرَ مُعَاذٌ عَنْهُ فَقَالَ إِنَّهُ مُنَافِقٌ . فَلَمَّا بَلَغَ ذَلِكَ الرَّجُلَ دَخَلَ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَأَخْبَرَهُ بِمَا قَالَ مُعَاذٌ . فَقَالَ لَهُ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " أَتُرِيدُ أَنْ تَكُونَ فَتَّانًا يَا مُعَاذُ إِذَا أَمَمْتَ النَّاسَ فَاقْرَأْ بِالشَّمْسِ وَضُحَاهَا وَ { سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الأَعْلَى } وَ { وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى } وَ { اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ }

Na amesema Qutaybah kua amesema Al Layth kua amesema Abu Zubayr kua amesema Jabr Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua:Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu*alisalisha Watu wake katika Sala ya Isha, na kisha ndani yake akasoma Sura Ndefu (Ambapo kuna Baadhi wanasema kua Alisoma Surat Al Baqara)

Hivyo mmoja kati ya Maamuma alipoona kua Muadh *Radhi Allahu Anhu* anasoma Sura ndefu, basi akakata Jamaa na kuamua Kusali peke yake. Kisha akamaliza kusali kabla ya Sala ya Jamaa na akatoka Msikitini na kuenda zake.

Na baada ya Sala watu wakamwambia Muadh kua kuna Mtu amekata Sala ya Jamaa na amesali peke yake. Muadh akasema kua: 'Mtu huyo ni Mnafiq'

Hivyo habari hizo za kuambiwa kwa Mtu huyo ni Mnafiq zilipomfika mwenyewe alieitwa Mnafiq kwa kukata Sala na Kusali peke yake. **Basi Mtu huyo akatoka na kuenda Kushtaki kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na aliyayasema Muadh juu yake baada ya Muadh Kusoma Sura ndefu na yeye akaamua Kukata Sala na kusali peke yake kwa Sababu ana shughuli nyengine ya kuwashughulikia Wanyama wake.**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwita Muadh aje kujibu Mashtaka hayo. **Na Muadh alipofika Mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kujieleza basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwangalia Muadh kisha akamwambia kwa kurudia Mara tatu kusema kua:Ewe Muadh! Jee unataka kuwafanyia Watu Mtihani katika dini yao?**

Ewe Muadh! Unaposalisha Watu katika Sala basi Soma Washamsi Wadhuhaha, Sabihisma Rabbika Al Aala, Walayli Ifha Yaghsha au Iqraa Biismi Rabbika*(Sunan An Nasai)*

Naam hivyo ndio maana Wanazuoni kama Imam An Nawawi, Imam Al Ramli, Imam Ibn Hajar Al Haythami n.k wakasema kua: '**Mtu anaesalisha wenzake hatakiwi kusoma Dhikr Allah zaidi ya 3 kwenye Rukuu na kwenye Sijda n.k**. **Isipokua pale itakapokua Wale anaowasalisha Wameridhika juu ya Kuirefusha Sala husika.'***(Al Majmuu, Nihayat Al Muhtaj na Tuhfah Al Muhtaj)*

Hivyo basi nawausia wale wanaosalisha kua Katika Kusalisha kwao Wanatakiwa wahakikishe kua Wanaposoma Sura ndefu basi iwe kuna Maridhiano kutoka kwa Maamuma, kwa sababu kama hakuna Maridhiano basi hua haikubaliki na hua ni sawa na Kuwafanyia watu ugumu katika Ibada na kusababisha Mitihani.Na hii ni kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni na pia kutokana uthibitisho wa Hadith ya Jabir kutokana na Muadh *Radhi Allahu Anhum* mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwani kuna baadhi wanaweza wakapingana na Mtizamo huo wa Imam Al Battal kwa kutoa Mfano wa Hadith ifuatayo:

خْبَرَنَا عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ مُحَمَّدِ بْنِ سَلاَّمٍ، قَالَ حَدَّثَنَا يَزِيدُ بْنُ هَارُونَ، قَالَ أَنْبَأَنَا جَرِيرُ بْنُ حَازِمٍ، قَالَ حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ أَبِي يَعْقُوبَ الْبَصْرِيُّ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ شَدَّادٍ، عَنْ أَبِيهِ، قَالَ خَرَجَ عَلَيْنَا رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فِي إِحْدَى صَلاَتَيِ الْعِشَاءِ وَهُوَ حَامِلٌ حَسَنًا أَوْ حُسَيْنًا فَتَقَدَّمَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَوَضَعَهُ ثُمَّ كَبَّرَ لِلصَّلاَةِ فَصَلَّى فَسَجَدَ بَيْنَ ظَهْرَانَىْ صَلاَتِهِ سَجْدَةً أَطَالَهَا . قَالَ أَبِي فَرَفَعْتُ رَأْسِي وَإِذَا الصَّبِيُّ عَلَى ظَهْرِ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم وَهُوَ سَاجِدٌ فَرَجَعْتُ إِلَى سُجُودِي فَلَمَّا قَضَى رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم الصَّلاَةَ قَالَ النَّاسُ يَا رَسُولَ اللَّهِ إِنَّكَ سَجَدْتَ بَيْنَ ظَهْرَانَىْ صَلاَتِكَ سَجْدَةً أَطَلْتَهَا حَتَّى ظَنَنَّا أَنَّهُ قَدْ حَدَثَ أَمْرٌ أَوْ أَنَّهُ يُوحَى إِلَيْكَ . قَالَ "كُلُّ ذَلِكَ لَمْ يَكُنْ وَلَكِنَّ ابْنِي ارْتَحَلَنِي فَكَرِهْتُ أَنْ أُعَجِّلَهُ حَتَّى يَقْضِيَ حَاجَتَهُ " .

Anasema Abd Allah Ibm Shaddad kua amesema Baba yake kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoka (kwake) na kuja kwetu sisi (Msikitini) kwa ajili ya Sala ya Isha,huku akiwa amembeba Hasan au Husein. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaja mbele yetu na akamshusha chini

Na kisha akasema Takbir na kuanza Kusalisha. Na katika Kusujudu kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi akaifanya Sijda hio kua ndefu sana.

Abd Allah Ibn Shaddad anaendelea kusema kua: Baba yangu akasema, Mimi nikanyanyua Kichwa na Nikamuona Mtoto akiwa juu ya Mgongo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*

Huku yeye *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa amesujudu, Hivyo na mimi nikarudi tena Katika Kusujudu.

Hivyo baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumaliza Kusalisha, basi watu wakasema:

Ya Rasul Allah! Hakika ukisujudu kwa mda mrefu sana kiasi ya kua sisi tulidhania kua labda kuna jambo limekutokea, au labda ulikua unashushiwa Wahyi

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu kwa kusema: La hakuna jambo kama hilo lililotokea isipokua Mjukuu wangu alikua amepanda Juu ya Mgongo wangu, hivyo nami sikutaka kumshughulisha hadi pale atakapotosheka kunipandia.' *(Imam An Nasai, Imam Ibn Asakir na Ima Al Hakim)*

Natunapoiangalia Hadith hii basi mbali ya kua inatuoneshaUmuhimu wa Kuwazoesha Watoto wetu kuenda Msikitini tangu wakiwa wadogo, ili wapate kuzoea na kukulia katika Mazingira ya kusimamia na kutekeleza Ibada ya Sala.

Lakini pia ndani yake tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alirefusha Sujud yake katika Sala hii ya Isha ambayo ni ya Jamaa Msikitini, kwa sababu ya kua Mjukuu wake amepanda juu ya Mgongo wake,

Na hivyo hakutaka kumlazimisha Mjukuu wake huyo kushuka na pia kwa sababu huenda kama angenyanyuka kutoka kwenye Sijjda hio basi Mjukuu wake huyo angeanguka na kuumia.

Na ndio maana akaamua kubakia katika hali ya Kuirefusha Sujud hio hadi Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakaanza kuingiwa na wasiwasi juu yake

Ambapo pia hili jambo la kuwatia wasiwasi Masahaba zake ndio pia jambo ambalo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hapendi litokee.Na ndio maana ikawa hataki kuwarefushia Masahaba zake Sala zao.

Kwani kwa upande mwengine basi kuna hadith ya Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* isemayo pia kua: ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anasali, na mara aliposujudu basi Hasan na Husein wakamrukia Juu ya Mgongo wake**

Na Masahaba wakataka kuwazuia Hasan na Huseinwasimpandie lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaashiria kua wawaachie.

Na baada ya Kusali basi *Rasul Allah Salallaju Alayhi wa Salam* akawachukua Hasan na Husein na kuwapakata na kisha akasema; Mwenye kunipenda Mimi anatakiwa awapende na hawa wawili pia.' *(Imam Ibn Khuzaymah)*

SIJDA YA PILI NA UKAMILIFU WA RAKAA.

❖❖❖

Tunarudi katika maneno ya*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomwambia Sahaba wake kuhusiana na Sujud kua:

ثم اسجد حتى تطمىءن ساجدا ثم ارفع حتى تسثوي وتطمىءن جالسا ثم اسجد حتى تطمىءن ساجد

Kisha Sujudu hadi Ujisikie Umetulia kwenye Sijda yako,na Kisha Nyanyuka Ukae kitako hadi ujisikie kua Umetulia katika Kukaa kwako,na Kisha Sujudu Tena hadi ujisikie kua Umetulia katika Sijda yako.

Kwani hadith hii ya *Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu* inatuonesha kua baada ya Kusujudu Mara ya kwanza na kisha Kukaa Kitako basi hua inabidi Kusujudu ili kukamilisha Rakaa husika ya Sala husika.

Kwani anasema Amam Al Muhaqqiqin Imam Ibn Hajar Al Haytami kua '**Kama ikiwa Mtu atasujudu Mara moja tu na kisha akainuka na Kusimama moja kwa Moja kwa makusudi basi Mtu huyo hua Hana Sala,kwa sababu hakukamilisha Sujud yake ambayo ni Nguzo ya Sala.Na hivyo hapo hapo anatakiwa arudi chini kwa ajili ya Kusujudu Sijda ya pili ili kutimiza Sijda za Rakaa husika kisha ndio anatakiwa anyanyuke juu tena na kusimama.**

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi mtu huyu pia itambidi Alete Sijda Sahw mwishoni mwa Sala yake, hata kama ikiwa mtu huyo akikukumbuka baadae kua kumbe ile aliyosujudu mwanzo ilikua ni Sijda ya pili na hivyo amesujudu mara tatu badala yake'*(Tuhfah Al Muhtaj)*

Ambapo Mtizamo huo pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa Madhhab ya Imam Hanbal na Imam Malik pia.*(Radd Al Mukhtar Ibn Abidin, Al Insaaf - Al Mardawi)*

Na hii pia ni kwa sababu kama Mtu akiwa hana uhakika wa kua amewacha Nguzo moja ya Sala ama la basi kisharia tunapozungumzia Sala hua ni Mwenye kuhseabiwa kua ameiwacha Nguzo hio,na hivyo kua ni mwenye kuharibu mpangalio wa Ibada yake na hua ni Wajibu kuirudia ili kukamilisha Ibada yake ya Sala.

Ambapo kwa Upande wa Imam Abu Ikhlas Hasan Ibn Ali Ibn Shurunbulali Al Wafai Al Hanafi basi yeye anasema kua: '**Kama Mtu ikiwa amesahau kua amesjudu mara moja ama mara mbili katika Rakaa basi anatakiwa asujudu tena mara ya pili, na hivyo hua hatakiwi kurudia Rakaa nzima kwa sababu Kupangalia Sujud kimpangilio hua ni Wajib tu'***(Maraqi Al Falah)*

Na anasema Imam Abu Bakr Ibn Ahmad Ibn Muhammad Al Adhram kua: '**Mimi nilimuuliza Abu Abd Allah kuhusiana na Mtu ambae amesali Rakaa ya kwanza na kisha akasimama kwa ajili ya RaKaa ya pili,na kisha akakumbuka kua kumbe katika Rakaa ya kwanza amesujudu mara moja tu. Jee atafanyeje?.'**

Ambapo nae akajibu Kama ikiwa hicho ndio kitu cha kwanza kukumbuka mara tu baada ya kusimama basi kabla hajafanya jambo lolote lile la Rakaa ya pili itambidi arudi chini akamalizie Sujud ya pili ya Rakaa ya kwanza.

Lakini kama ikiwa tayari ameshaanza kisomo cha Rakaa ya pili, basi hii Rakaa ya pili ndio itakua Rakaa yake ya kwanza ndani ya Sala hio, na huifuta ile iliyotangulia' *(Matalib Ul Nuha)*

Hivyo Wanasema Wanazuoni kua : '**Yeyote yule aliesahau Kusujudu Sijda ya Pili ya Rakaa basi hua ni Lazima kwake Kuitekeleza Sijda hio pale pale atakapokumbuka kabla hajaingia katika**

Rakaa inayofuatia. Na kama ikiwa ameshaingia katika Rakaa inayofuatia basi humbidi kuibatilisha ile Rakaa iliyotangulia kutokana na Kasoro yake.'

'Na hivyo mtu husika Humbidi kuhesabu Rakaa aliyomo kua ndio Rakaa sahih. Na kwa maana hio basi kama Mtu anasali na kisha alipofika Rakaa ya pili katika kusujudu akakumbuka kua kumbe katika Rakaa ya kwanza alirukuu mara moja tu.'

Basi hapa itambidi hii Rakaa yake ya pili ndio aihesabu kua ndio Rakaa ya Kwanza.

Na itakapokua hakuwahi kukumbuka juu ya kasoro ya Rakaa moja hio hadi pale alipomaliza Kusali, basi kwa kua hujapita mda mrefu tangu kutoa Salam basi Mtu huyo humbidi kuiongezea Rakaa moja hio iliyokua na kasoro, kukaa *Attahiyat* na kisha kutoa Salam na kumalizia Sala yake hio.'

Kwani hii pia ni kulingana na Hadith ya *Dhu Al Yadayn* tuliyoizungumzia hapo mwanzoni mwa Mada hii ambayo inasema kua:

Abd Allah Ibn Yusuf kua amesema Malik Ibn Anas kua amesema Ayoub Al Sakhtiyani kua:

عن أبي هُرَيرَة رَضِيَ اللهُ عَنْه، قال صلَّى بنا رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم إحْدَى صلاتَيِ العشيِّ – سمَّاها أبو هريرة، ولكن نسيتُ أنا– قال: فصلَّى بنا ركعتينِ، ثم سلَّمَ، فقام إلى :قال ابن سِيرين خشبةٍ معروضةٍ في المسجِدِ، فاتَّكأَ عليها كأنَّه غَضبانُ، ووضَعَ يَدَه اليُمنى على اليُسرى، وشبَّكَ بين أصابعِه، ووَضَع خَدَّه الأيمنَ على ظَهرِ كفِّه اليُسرى، وخرَجتِ السَّرَعانُ من أبوابِ المسجدِ، فقالوا: وعُمرُ، فهابَا أن يُكلِّماه، وفي القومِ رجلٌ في يديه طولٌ، يُقال قَصُرتِ الصَّلاةُ؟ وفي القومِ أبو بكرٍ له: ذو اليَدينِ، قال: يا رسولَ الله، أَنسيتَ أمْ قَصُرَتِ الصَّلاةُ؟ قال: لم أَنسَ ولم تَقصُر! فقال: أكَمَا يقولُ ذو اليدين؟ فقالوا: نعَمْ، فتقدَّم فصلَّى ما تَرَك، ثم سَلَّم، ثم كَبَّر وسجَدَ مِثلَ سُجودِه أو أطولَ، ثم رفَعَ رأسَه وكبَّر، ثم كبَّر وسَجَد مِثلَ سجودِه أو أطولَ، ثم رفَع رأسَه وكبَّر. فربَّما سألوه (أي: سألوا ابنَ سيرينثم سلَّم؟ فيقول: نُبِّئتُ أنَّ عِمران بن حُصَينٍ، قال: ثم سَلَّمَ

Amesema Muhammad Ibn Sirin kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha moja kati ya Sala za Jioni (Ambapo Imam Ibn Sirin anasema kua Abu Hurayrah Aliitaja Sala hio ila mimi nimeisahau) na akaihitimisha Sala hio baada ya Kuisalisha kwa Rakaa mbili tu. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka na kusimama kwenye karibu na Kigogo kilichopo mbele ya Msikiti na kuuweka mkono wake juu yake huku akiwa anaonekana kama kwamba amekasirika, akauweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto na kuvipitisha vidole vyake vya kulia baina ya vidole vyake vya kulia.

Ambapo Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* hawakuweza kusema chochote kutokana na kumuogopa na kumuheshimu *Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam*. Na wale Masahaba

waliokua na Haraka wakaharakisha kutoka Nje, **Huku wakiulizana kwa kusema: 'Vipi Leo Sala imefupishwa au?'**

Hivyo Kuna Mtu aitwae Dhu Al Yadayn akamsogelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuuliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah Hivi Leo Sala Imefupishwa au umesahau?'

***Rasul Allah Sallallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La Haikufupishwa na wala Sikusahau.'**

Dhu Al Yadayn *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama haikufupishwa basi kwa hakika itakua Umesahau.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum:*'Hivi Jee Dhu Al Yadayn anasema kweli ama la?'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Naam, anasema Ukweli'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasimama. **Na kusalisha Rakaa mbili zilizobakia ambazo alizisahau, na kisha akatoa Salam na akasema Allahu Akbar na kusjudu Sijdat ya Sahau ilizochukua mda wa kama Sijda za Kawaida au zaidi kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar na kisha Akasema Allahu Akbar na Kusujud tena Sijda ya pili na kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akba**r.'

Ambapo Imam Muhammad Ibn Sirin alipoulizwa kuhusiana na kua 'Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam kumalizia ama la?'

Basi Imam Muhammad Ibn Sirin akasema kua: 'Mimi nimeambiwa na Imran Ibn Husayn *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam'*(Bukhari na Muslim)*

Ambapo huu ndio Mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Malik, Imam Al Layth, Imam Al Awzai, Imam Yahya Al Ansari n.k

Ambapo Imam Muhammad Idris Al Shafi anasema kua: **Kama Mtu atakua ameshau Nguzo miongoni mwa nguzo za Sala, na kisha baada ya Kumaliza kusali akakumbuka huku ukiwa umeshapita Mda mrefu basi Mtu huyo humbidi Kuirudia Sala hio**. **Ama ikiwa haujapita Mda mrefu na Udhu wake anao basi haina haja kwake kuirudia Sala yote bali hua inambidi kuirudia Rakaa moja aliyoikosea***(Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi)*

Kwani inasema Majmua Al Buhuth Al Islamiyah Ambayo ni Tasisi ya uchunguzi ya Fatwa za Chuo kikuu cha Al Azhar ya Misri kua: '**Ama kuhusiana na Mtu atakaesahau kusujudu katika Rakaa, basi kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Hanbal wanasema kua:**

Basi ni Wajibu kwake kuirudia Rakaa hio na kama hakufanya hivyo na Mda mrefu ukawa umeshapita basi Sala yake hua ni Batili,na ni lazima kwake kuirudia Sala yote nzima badala yake Na kama Mtu ikiwa amesahau Kujusudu Sijda ya pili katika Rakaa ya mwisho na hivyo baada ya Sijda ya kwanza ya Rakaa ya mwisho ik**awa amekaa kitako na kuanza kusoma Attahiyat na kisha kabla ya kutoa Salam akakumbuka kua kumbe alisujudu Mara moja tu.**

Basi kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhab ya Imam Al Shafii basi ni kua kabla ya kuendelea zaidi basi hapo hapo alipofikia atasujudu, kisha atasoma Attahiyat

na kutoa Salam bila kuirudia Rakaa, ila atatekeleza na Sijda Sahaw pia. **Na hii ni kwa sababu katika hili hua Sijdat Sahaw peke yake haitoshelezi bali ni lazima Airudie Sijda hio aliyoiacha***(Majmua Al Buhuth Al Islamiya)*

HIKMA YA KURUDIA RUDIA HATUA ZA KILA RAKAA YA SALA

❖❖❖

Kwani katika kuangalia kuhusiana na hatua kwa hatua za ndani ya Ibada ya Sala basi tumeona kua kuna marudio ya kila hatua ya Sala katika Kila Rakaa ya Sala.

Na kuna baadhi ya Hatua ambazo inabidi katika kila Rakaa zirudiwe mara mbili. Kiasi ya kua kama hatua husika ukiitekeleza mara moja tu basi hua haitoshelezi ambapo miongoni mwao ni kama tulivyoona kwenye Hatua ya Kusujudu.

Kwani unapotafakkar kuhusiana na mfumo huu wa kurudia rudia Hatua za Ibada ya Sala basi utaona kua ndani yake kuna Hikma na mafunzo mengi sana ikiwemo Ile yenye kutuonesha kua Kama ilivyo Ibada ya Sala basi ndivyo yalivyo maisha yetu pia kua ni yenye kuendelea kutokana na Siku na Matukio yanayojirejea rejea ndani yake.

Na hivyo ili Ibn Adam tuweze kua ni wenye kupata Mafanikio basi hatuna budi Kuzizoesha Nafsi zetu na Nyoyo zetu kila wakati kufanya Mema na kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuweza kurudi kwake bila ya kujali kasoro zetu kwani Rehma na Maghfira ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Makubwa Sana. Kwani anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kua:

﴿إِنَّ رَحْمَةَ ٱللَّهِ قَرِيبٌ مِّنَ ٱلْمُحْسِنِينَ﴾

Inna rahmata Allahi qareebun mina almuhsineena*(Surat Al Aaraf 7:56)*

*Tafsir:**Hakika ya Rehma za Allah Ziko Karibu sana kwa wenye Kufanya Mema***

Ambapo amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua; '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa *Salam* kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* amejaalia Rehma zake kua katika sehemu 100, kisha sehemu 99 akazifunga, na kuchukua sehemu Moja iliyobakia na kuishusha Ulimwenguni**. **Ili Viumbe wa Ulimwenguni wapate kupendana kwa kufikia hali ya kua hata Farasi hua ni mwenye kunyanyua Mguu wake ili asimkanyage Mtoto wake'***(Imam Al Samarqandi)*

Na akasema tena Imam Al Layth al Samarqandi kua: '**Amesema Al Hasan kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:Kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuna sehemu 100 za Rehma ambapo miongoni mwao basi ni sehemu Moja tu ndio waliopewa Viumbe wanaoishi Ulimwenguni. Na ingawa ni hio Moja tu basi lakini hua ni yenye kumtosheleza kila Mtu hadi mwisho wa Uhai Wake**. **Ambapo Katika Siku ya Malipo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atazirudisha Rehma zake**. **Katika hali yake kamilifu ya sehemu 100, na kisha Atawamwagia Waja wake awapendao na wale waliokua wakijitolea kwa ajili yake.'**

Kwani Hatua za Ibada ya Sala inatufundisha kutosahau juu ya Hatua za kurudi kwa Mola wetu kila mara kwani Anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿نَبِّىٔۡ عِبَادِىٓ أَنِّيٓ أَنَا ٱلۡغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ ۝ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ ٱلۡعَذَابُ ٱلۡأَلِيمُ﴾

Nabbi/ AAibadee annee ana alghafooru alrraheemu; Waanna AAadhabee huwa alAAadhabu Al aleemu*(Surat Al Hijr 15:49-50)*

Tafsir: **Waafikishie Waja wangu kua mimi ni mwingi wa Usamehevu na Mwingi wa Rehma**. **Na Adhabu yangu ni Adhabu kali sana**

Na akasema tena kua:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّٰبِينَ وَيُحِبُّ ٱلۡمُتَطَهِّرِينَ﴾

Inna Allaha yuhibbu alttawwabeena wayuhibbu almutatahhireena*(Surat Al Baqara 2:222)*

Tafsir **- *Hakika Allah Anawapenda wale Wanaorudia rudia Kutubu kwake na anawapenda Wanaojitoharisha***

Kwani bila ya Shaka hali ipo kama alivyosema Imam Hasan Al Basr alipoulizwa kua: '**Hivi Jee Sisi Kila Siku tunafanya Dhambi hatuoni Haya Kila Siku Kumuomba msamaha *Allah Subhanah wa Ta'ala?'***

Ambapo Imam Hasan Al Basr akajibu kwa kusema: '**Ibilis anataka hasa kua Muone haya kuomba Msamaha wa Mola wenu kila Mara, Hivyo Msichoke kuomba Msamaha.'**

Kwani anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu kua:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسۡتَقَٰمُواْ تَتَنَزَّلُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُواْ﴾

Inna alladheena qaloo rabbuna Allahu thumma istaqamoo tatanazzalu AAalayhimu almalaikatu alla takhafoo wala tahzanoo waabshiroo bialjannati allatee kuntum tooAAadoona*(Surat Fussilat 41:30)*

*Tafsir:****Hakika ya Wale wanaosema kua Mola wetu ni AllahNa Kisha wakawa na Msimamo basi Hushukiwa na Malaika Wakiwaambia Msiwe na Khofu wa Huzunina Pokeeni Habari Njema za Pepo Ambayo Mmeahidiwa.***

Ambapo Aya hii inatuonesha na kutusisitizia kuhusiana na Umuhimu wa kua na Msiamamo mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Katika kumuamini na Kumuabudu ipasavyo kua kwa kila mwenye kufanya hivyo basi hua hakuna kua na Khofu kwake wala Huzuni.

Na anasema *Mujaddid Ad Din* Imam Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na aya hii kua: '**Kutokua na Khofu wala Huzuni huko kunakozungumziwa hapa, ni katika Matukio matatu yenye kutisha sana kwa Kila Ibn Adam ambayo ni:** '**Katika Wakati wa Kukata Roho, Katika Wakati wa Kukaa Kaburini na Katika wakati wa Kufufuliwa.'**

Ambapo kuhusiana na hali za Khofu na Huzuni basi anasema Imam Mujahid Ibn Sulayman na Imam Abd Rahman Al Suddi Kua: '**Wataambiwa kua Wasiwe na Khofu juu ya yatakayotokea hapo baadae na wala wasiwe na Huzuni juu ya Yaliyopita.'**

Ambapo Kimaumbile hisia za Khofu hua ni Kuhusiana na Kile ambacho hakijatokea na hakijulikani itakuaje katika kutokea kwake.Wakati hisia za Huzuni Kimaumbile hua ni zenye kuhusisha kile kitu ambacho kimeshatokea hapo kabla.Na bila ya shaka Hisia za Khofu hua ni zenye nguvu na kubwa zaid kuliko za huzuni na ndio maana katika aya ikataja Khofu kwanza kisha ikataja Huzuni.

Hivyo tukirudi katika Kurudia rudi hatua zilizomo ndani ya kila rakaa za Sala, na kutafakkari maneno ya Aya hii basi tunaona kua ndani yake mna Hikam ioneshayo kua**: 'Mpangilio wa marudio rudio ya Hatua za Kila Rakaa ya Sala unatufunzakua na Msimamo katika kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na hivyo basi hua hatutakiwi kuvunjika Moyo, au kukata Tamaa,Kuona Uvivu au Kuchoka bali tunatakiwa tushikamane na Ibada ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kadri tutakavyoweza hadi mwisho wa Uhai wetu hapa Duniani.'**

Kwani ni kutokana na kua na Msimamo huo tu, ndiko kutakako tupelekea kufuzu katika Kufikia Malengo ya Kuumbwa kwetu. Jambo ambalo ndio litakalotupelekea kuingizwa kwenye Hali ya kutokua na Khofu wala Huzuni

Ama tunapoangalia zaid basi tunaona kua miongoni mwa Hikma zilizomo ndani yake hatua hii Kurudiwa mara mbili basi hua ni kama alivyosema

Rabiah Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* ambae anasema kua:

كُنْتُ أَبِيتُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَأَتَيْتُهُ بِوَضُوئِهِ وَحَاجَتِهِ فَقَالَ لِي: «سَلْ» فَقُلْتُ: أَسْأَلُكَ مُرَافَقَتَكَ فِي الْجَنَّةِ. قَالَ: «أَو غير ذَلِكَ؟» . قُلْتُ هُوَ ذَاكَ. قَالَ: «فَأَعِنِّي عَلَى نَفسك بِكَثْرَة السُّجُود»

Mimi nilikua na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika wakati wa Usiku ambapo nilimpelekea Maji ya kutilia Udhu, na nilipomfikishia Maji hayo basi akaniambia:

'Omba Unachotaka'

Nami nikasema Mimi 'Naomba Kua niwe pamoja nawe Peponi.'

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Jee huna Ombi Jengine zaidi?

Nami nikasema 'La Ombi langu ni hilo tu.'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kama ni hivyo basi nisaidie Mimi kukutekelezea hilo kwa kujitolea mara kwa mara kua ni mwenye Kusujudu.'(Sahih Muslim)*

Na pia amesema Madan Ibn Talha kua:

لَقِيتُ ثَوْبَانَ مَوْلَى رَسولِ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ، فَقُلتُ: أَخْبِرْنِي بعَمَلٍ أعْمَلُهُ يُدْخِلُنِي اللَّهُ به الجَنَّةَ؟ أوْ قالَ قُلتُ: بأَحَبِّ الأعْمَالِ إلى اللهِ، فَسَكَتَ. ثُمَّ سَأَلْتُهُ فَسَكَتَ. ثُمَّ سَأَلْتُهُ الثَّالِثَةَ فَقالَ: سَأَلْتُ عن

ذلكَ رَسولَ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ، فَقالَ: عَلَيْكَ بكَثْرَةِ السُّجُودِ لِلَّهِ، فإنَّكَ لا تَسْجُدُ لِلَّهِ سَجْدَةً، إلَّا رَفَعَكَ اللَّهُ بهَا دَرَجَةً، وحَطَّ عَنْكَ بهَا خَطِيئَةً

Mimi nimekutana na Thawban aliekua Mtumwa wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha akaachiwa huru nae.Na nikamuuliza kuhusiana na Amali ambayo kama nitaifanya basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ataniingiza Peponi

Yaani Amali ambayo inapendwa zaidi na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo hata hivyo nae hakunipa Jibu, hivyo nikamuuliza tena lakini hakunijibu, na kisha nikamuuliza tena mara ya tatu ambapo nae akasema: 'Hakika mimi nilimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Suali hilo,nae akaniambia kua: Fanya Sijda nyingi sana mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwani hutofanya Sijda hata Moja bila ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua ni Mwenye kukupandisha Darja kwa sababu ya Sijda hio na pia kua ni mwenye Kukufutia Dhambi kutokana na Sijda hio.

Baada ya Madan kumuuliza Thawba suali hilo na kupewa Jibu hilo basi akakutana na Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* na kumuuliza Suali hilo pia anaendelea kua: Na nikakutana na Abu Dardaa na nilipomuuliza juu ya Suali hilo basi nae akaniambia Hivyo hivyo.*(Sahih Muslim)*

Kwa maana hio basi Wingi wa Kurudiwa kwa Sijda ndani ya Sala hua pia ni Kupandishwa Darja zaid kwa kila Sijida mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na pia hua ni sehemu ya Kufutiwa Dhambi zetu kwa Wingi zaidi pia kwa kila Ibada ya Sala.

MAVAZI YA YANAYOBATILISHA SUJUD.

❖❖❖

Mara nyingi sana katika wakati wetu kuna aina za Mavazi ambayo hua ni yenye kupendwa sana na Vijana mbali mbali wakiwemo wa Kiislam.Kiasi ya kua unaweza kumkuta Mtu ameingia Msikitini huku akiwa amevaa Suruali Inambana au imeshuka hadi chini ya Makalio au Shati, Fulana inambana na pia ni Fupi sana kiasi ya kua akisujudu basi sehemu yaMpasuko wa Makalio hua Inaonekana au sehemu ya chini ya Uti wa Mgongo inaonekana.

Ambapo hili ni jambo ambalo halifai hususan pale Mtu unapokua umejitayarisha kwa ajili ya Kumsujudia Mola wako. Kwani Kiislam sehemu hizo za mwili hua zinahesabika kua ni sehemu za Siri ambazo zitakakiwa kusitiriwa. Na moja kati ya Masharti ya Kukubalika kwa Ibada ya Sala basi ni kua Mtu anaesali anatakiwa awe ni mwenye kujihifadhi na sehemu zake za Siri.

Isipokua pale inapokua kuna Udhuru unaokubalika Kisharia.Na kuhusiana na Aina za Udhuru basi tutafahamisha katika Kurasa za Mbele tutakapozungumzia kuhusiana na Mavazi stahiki ndani ya Sala.Na siwezi kuzungumzia hapa kwa sababu hapa bado tupo kwenye hatua Sujud, ambapo inanibidi nizungumzie yanayobatilisha Sujud ya Mtu katika Sala.

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kujihifadhi Sehemu za Siri hua ni Sharti la Kukubaliwa kwa Sala Husika.Hivyo Kama ikiwa sehemu ya Siri itaonekana basi Sala ya Mtu husika Hubatilika.Iwe sehemu hio ni Ndogo ama Kubwa, kwani hata ile sehemu ndogo tu ya Mtu anaesali**. **Iwe Mwanamme au Mwanamke, iwe Sala ya Jamaa Au Sala ya Mtu Peke yake, iwe Sala ya Sunna au ya Fardhi au Sala ya Maiti, iwe Tawaf au Sujd At Tilawah ndani ya Sala.'***(Al Majmuu)*

Kwa maana hio basi kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii tunaina kua kama ikiwa Mtu atasujuduna kisha Fulana au Shati yake ikapanda Juu. Na kuachia Wazi sehemu ya Mwili wake ambayo iko zaidi ya chini ya Kitovu,basi Sala hio Hua Ni Batili na Hubidi Kurudiwa tena Upya. Yaani inayobatilika si Sujud peke yake bali ni Sala nzima.

Hivyo kwa Kila Muislam hua ni Wajibu kuhakikisha kua nguo anazovaa zinamhifadhi vizuri na ipasavyo kama kweli ni mwenye Kusali kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* au la Sivyo Sala yote itakua Bure.Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Awra au Uchi wa Mwanamme Ndani ya Sala hua ni kuanzia Juu ya Kitovu hafi chini ya Magoti

Na Uchi wa Mwanamke Ndani ya Sala hua ni Mwili wake wote isipokua Uso wake na Mikono yake. Kwa maana hio kama ikiwa Mtu Mwanamme atasujudu na kisha Shati lake likapanda Juu kiunoni kutokana na Ufupi wake au kaa bahati mbaya na kuonesha sehemu ya Uchi wake,, basi Sala ya Mwanamme husika Itabatilika pale itakapokua Muonekano wa sehemu hio isiyotakiwa kuonekana yaani ya Uchi kuonekana kwa zaidi ya sekunde 4 Yaani Zaidi ya mda wa kusema *Subhanah Rabbi Al Aala* mara 3 na ikizidi mara ya 4 basi Sala itabatilika

Lakini kama ikiwa umeonekana kwa mda wa chini ya mda huo na mwenye Kusali akawahi Kujifunika au kujiziba basi Sala hua haijabatilika

Kwani hukmu hii pia inaenda sambamba na kwa upande wa Mwanamke piaYaani ikitokea kwa bahati mbaya au kwa makusudi Mtu Mwanamke anaesali akawacha wazi sehemu ya mwili sake inayohesabika kua ni Uchi ndani ya Sala yake basi na pia Sala yake itabatilika kama ikiwa Muonekano huo wa sehemu hio umezidi zaidi ya kusema *Subhanah Rabbi Al Aala* mara 3.

Lakini kama ikiwa haukufikia mda huo na akawahi kujifunika basi Sala yake hua haijabatilika, kwa maana hio basi kama sehemu ya Mwili inayotakiwa kuhifadhiwa ya Mtu anaesali ikawa iko katika hali ya kutohifadhiwa au iko wazi na Mtu husika hakuwahi kuiziba au kuifunika kwa haraka ndani ya wakati, basi Sala hubatilika kutokana na kuwepo kwa hali ya Kutojali kwa Mtu husika kua yuko Mbele ya Mola wake na anatakiwa Ajihifadhi na pia Kutokua na Umakini na hivyo kutoitilia maanani Ibada ya Sala yake husika

Kwani kutokana na kutojali kwake huko basi Sala ya Mtu husika hua ni sawa na Sala ya wale waliotajwa katika Aya zisemazo:

﴿ فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ۞ ٱلَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ﴾

Fawaylun lilmu<u>s</u>alleena; Alla<u>dh</u>eena hum AAan <u>s</u>al<u>a</u>tihim s<u>a</u>hoona; *(Surat Al Maun 107:5-6)*

Tafsir: ***Hivyo Ole wao Wale Wanaosali; Wale Ambao Kuhusiana na Sala zao hua Wanazidharau na kutozijali.***

Kwani kwa maana hio basi Sehemu za Siri za Mwanamme ambazo zinatakiwa Kuhifadhiwa Hususan Ndani ya Sala hua ni zifuatazo:

1-Sehemu Zote za Viungo vya Uzazi.

2-Tupu za Mbele na za Nyuma

3- Makalio - ambapo Kila Kalio hua ni sehemu inayojitegemea, yaani sio kama ikiwa limeonekana Moja basi hamna tatizo, mpaka yaonekane yote mawili ndio tatizo, La hali haiku hivyo kwani likionekana moja tu basi unabatilisha Sijida yako na Sala yako yote hapo hapo.

4-Mapaja na Magoti ambapo kila Moja linajitegemea pia kama ilivyo kwa Makalio.

5-Kuanzia Kitovuni kushuka chini hadi juu ya sehemu za Siri, kwa upande wa Mbele, Nyuma, na pande zote mbili za Kulia na Kushoto-Ambazo hizi ndio mara nyingi hua zinaonekana na kwa Wale wanaovaa Nguo fupi za Juu katika wakati wa Kusujudi

Ambapo kwa Upande wa Wanawake basi sehemu zao za Siri hua ni:

1-Sehemu zote za Viungo vya Uzazi.

2-Sehemu za Siri za Mbele na Nyuma.

3-Makalio, ambapo Kila Kalio hua ni sehemu inayojitegemea.

4- Mapaja na Magoti yote mawili na kila moja ni sehemu inayojitegemea.

5-Kuanzia Kitovuni hadi Juu ya sehemu za Siri, kwa mbele, kwa nyuma, kushoto na Kulia pia.

6-Viungio vya chini vya Miguu ambapo kila kimoja kinajitegemea.

7-Maziwa, ambapo Kila Ziwa hua ni sehemu inayojitegemea.

8-Masikio ambapo kila sikio hua ni sehemu inayojitegemea.

9-Mikono kuanzia Juu hadi kwenye visugudi, na kila sehemu inajitegemea.

10-Mikono Kuanzia kwenye Visugudi hadi kwenye kiungio cha Viganja, na kila kimoja kinajitegemea.

11-Mabega.

12-Shingo.

13-Kichwa.

14-Nywele.

Naam..hivyo ndio viungo vinavyotakiwa kuhifadhiwa kwa upande wa Mwanamme na Mwanammke hususan unapokua ndani ya Sala.

Hivyo kuiwacha wazi sehemu ndogo tu kati ya Viungo hivyo kutokana na kudharau na kutojalia basi hua kunapelekea Sala ya Mtu kua ni Batili.

Na kama tulivyosema kua mara nyingi sana katika Nyakati za Kusujudu kwa wanaovaa Nguo fupi za Juu basi hua ni zenye kupanda na kuacha wazi sehemu zinazohesabika kua ni Uchi.Halafu

unakuta kua Mtu hata habari hana wala hahisi mabadiliko ya mazingira ya nyuma kwake na anaendelea na Sujud yake ya kwanza ya pili na kumalizia Sala yake, na kila akisujudu anaoonesha tena upya sehemu ya juu ya makalio yake na kujihesabu kua amesujudu na kumuabudu Mola wake.

HUKMU YA KUONEKANA KWA MIGUU YA MWANAMKE KATIKA SUJUD

Naam tumeona kuhusiana na Kasoro zinazodharaulika kwa upande wa Wanaume katika Sijda zao ndani ya Sala kutokana na Kuvaa Nguo Fupi kuwacha wazo sehemu zinazotakiwa kufunikwa na Hukmu yake kua ni Jambo lenye kubatilisha Sala.

Hivyo na tuangalie kwa Wanawake ambapo baadhi yao pia hudharau kuhusiana na Urefu wa Mavazi na kuacha wazi Miguu yao au nyayo zao. Kwani aliulizwa Ummu Ul Muuminina Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* kwa kuambiwa kua: **Hivi jee Mwanammke anaweza Kusali wakati Akiwa Amevaa Hijabu na Dira bila kuvaa Nguo Chini?**

Ambapo Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* akajibu: Naam Kama Dira hilo Likiwa ni Pana na Refu litakalofunika Miguu yake*(Sunan Abu Daud)*

Ambapo kwanza kabla hatujaendelea basi tufahamishane kuhusiana na Dira hua ndio Vazi gani, ili Watu wasije wakadhania vyengine.Dira ni Vazi ambalo hua linalivaliwa kwa ajili ya Kuihifadhi sehemu ya Juu ya Mwili kutokana na Madhara mbali mbali.Kwa maana hio basi Dira lililozungumziwa hapa hua ni aina ya Nguo ya Kike kama Shati Au Fulana yenye Mikono mirefu.

Na bila ya shaka kwa kua Ummu Salama *RadhiAllahu Anha* katoa sharti la kua Dira hili liatakiwa Liwe Pana na Refu litakalofunika Miguu kutokana na Urefu wake, basi hii inamaanisha kua Kuna Dira Fupi na Kuna Dira Refu.

Kwani anasema Imam Abu Sulayman Hamd Ibn Muhammad Ibm Ibrahim Al Khattabi Al Busti Al Shafii kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hadith hii ni yenye kutoa Uthibitisho unaoonesha kua Sala ya Mwanammke hua inabatilika kama ikiwa sehemu ya Mwili wake itakua Inaonekana, Hivyo ya Kusalia Mwanammke Nguo Inatakiwa Iwe Pana na yenye kufunika Miguu yake, hivyo kwa Mwanammke basi moja kati ya Masharti la Kukubalika Sala yake hua ni Kujihifadhi MwiliWake wote'***(Maalim Al Sunnan)*

Na ingawa huo ndio Mtizamo wa Imam Al Khattabi Al Busti Al Shafii kulingana na Hadith hii,lakini pia Mtizamo huo si Mtizamo wa Imam Al Khattabi peke yake.Kwani anasema Imam Muwaffaq Ad Din Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Imam Malik, Imam Al Awzai na Imam Al Shafii wote wamesema kua Sehemu zote za Mwili wa Mwanammke hua ni Uchi. Isipokua Uso wake na Viganja vya Mikono yake, na hivyo basi sehemu nyengine zote zilizobakia za Mwili wake zinatakiwa kuhifadhiwa pale anapokua ndani ya Ibada ya Sala.'***(Al Mughni)*

Na Mtizamo huu wa kua Sehemu zote za Mwili wa Mwanammke kua ni sehemu za Siri na hivyo zinatakiwa zihifadhiwe ndani ya Sala. Ndio Mtizamo ambao inakubaliwa na Wanazuoni wengi zaidi wa Madhhab Tofauti.

Na hii ni kwa sababu kuna Mtizamo mwengine pia ambao ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Al Muzani Al Shafii na Imam Sufyan Ath Thawry ambao wao wanasema

kua:**‘Mwanammke anapokua Katika Sala anatakiwa ajihifadhi Mwili mzima isipokua Uso na Viganja vya Mikono, na kwa Upande wa Miguu basi sila lazima kwani Miguu hua ni sawa na Uso na Viganja.’**

Na hivyo hii kuonesha pia kuna kutofautiana baina ya Wanazuoni kuhusiana na Miguu na Nyayo za Mwanammke kua kama ni sehemu ya Awra au Uchi yaani sehemu isiyotakiwa kuonekana ya Mwanammke wakati akiwa ndani ya Sala ama la. Kwani mbali ya kua kuna uthibitisho wa Hadith ya Dira ya Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* kama tulivyoiona hapo kabla.

Lakini pia kwa upande mwengine basi tuonaona kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: ‘**Kuhusiana na maneno ya Aya isemayo:**

﴿ وَقُل لِّلْمُؤْمِنَاتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَارِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلاَ يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلاَّ مَا ظَهَرَ مِنْهَا﴾

Wa Qul Al Muuminati Yaghdhudhna Min Abssarihina Wayahfadhna Furuujahunnawala yubdiina ziinatahuna illa ma dhahara minha*(Surat Nur 24:31)*

*Tafsir: **Na Waambie Waumini wanawake Wainamishe Chini Mtizamo wa Macho yao Na Wahifadhi Sehemu zao za Siri Na Wala Wasioeneshe Mapambo yaoIsipokua Yale Yaliyodhahirika kuonekana***

Hivyo Maneno Yaliyodhihirika kuonekana yanajumuisha Mapambo yanayovaliwa Kama Bangili za Mikononi na Pete za Kidole Gumba cha Mguuni.’

Hivyo Imam Sufyan Atha Thawry, Imam Al Muzani, Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wamekhitimisha kua Kwa Maana hio basi Miguu ha Mwanammke hua si Lazima Kufunikwa katika Sala kwa sababu si Awra.’*(Durr Al Mukhtar,Al Hidaya)*

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Shaykh Ibn Taymiyyah pale aliposema kua: ‘**Wanawake hawakuamrishwa Wazibe Miguu yao kwa Soksi au Viatu, na wala hawakuamrishwa kua Wavae soksi za mikononi au Wajifunike kitu chochote cha aina hio katika sehemu hizo, kwa Maana hio basi hii inathibitisha kua haina haja kwao kufunika Miguu yao wala Mikono yao katika Wakati wa Sala, labda pale itakapokua kuna Wanaume wasiowajua karibu yao.’**

Hivyo kuwaamrisha Wanawake kujifunika mikono na miguu ni kuvuka mipaka, kwani Wanawake wanaporukuu na kusujudu, Hurukuu kwa Kutumia Mikono pia na Husujudu kwa kutumia mikono pia kama vile ambavyo katika wakati wa Kipindi cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Wanawake walikua wakijisitiri kwa Mavazi yao, lakini mikono yao hua ni yenye kuonekana katika Shughuli zao za Kusaga Unga, Kukanda Unga, Kuchoma Mikate n.k

Hivyo Kama Mikono ingekua Lazima ifunikwe kwenye Sala basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angesema hivyo na kwa upande wa Miguu pia ndio hivyo hivyo’*(Fatawa Al Muslimat -Ibn Taymiyyah)*

Hivyo kwa Upande wa Shaykh Ibn Taymiyyah ambae ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn HanbalKua tunaona pia kuhusiana na Jambo hili basi ametoka nje ya Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kimtizamo kuhusiana na Jambo hili, kama ilivyokua kwa upande kwa Imam Al Muzani tulivyoona kua ametoka katika Madhhab Ya Imam Al Shafii Kimtizamo juu ya Jambo hili na kua na Mtizamo wake unaojitegemea.

Kwani kwa Upande wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii basi anasema Imam Muhammad Idris Al Shafii Mwenyewe katika Kitabu chake cha Al Umm kua: '**Kila sehemu ya Mwili wa Mwanammke ndani ya Sala hua ni Uchi isipokua Uso na Mikono, na hata Nyayo zake Mwanammke hua ni Uchi na hazitakiwi zionekane ndani ya Sala.'**

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik Ibn Anas basi anasema ImamIbn Abi Zayd Al Qayrawni katika Al Anwar wal Ziyadah kua: '**Mwanamke wa Kiislam asiekua Mtumwa anatakiwa Kusali huku akiaa amevaa Nguo pana na Ndefu ambayo itafunika Sehemu ya Nyuma ya Miguu yake katika Wakati wa Kurukuu na Kusjudu. Na pia anatakiwa awe amevaa Khimar (Mtandio) ambayo itamfunika Mabega yake na kutoonesha sehemu yeyote ya Mwili wake isipokua Uso wake na Mikono yake.'**

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal mwenyewe kua: '**Mwanamke anapokua anasali basi anatakiwa awe amevaa Nguo Ndefu na Khimar, na hivyo nguo hio inatakiwa iwe ndefu kiasi ya kua ni yenyw kufunika Miguu yake**(Masail Ibn Hani)

Hivyo tunamalizana na mada hiikwa kukumbashana kua Kwa Mwanamme wa Kiislam anapokua anasali basi anatakiwa aweAmevaa Nguo ndefu ya Juu ambayo haitovutika katika wakati wa Rukuu na Sujud na kuwacha wazi sehemu zinazotakiwa kuhifadhiwa.

Na pia kwa upande wa Mwanammke wa Kiislam anaposali basi nae pia anataiiwa Avae Nguo ndefu ambayo hata katika Wakati wa Kurukuu na Kusujudu haitowacha Wazi Miguu yake ama Nyayo zake Hivyo kwa Wanaume kama ikiwa Mtu amevaa Fulana ya Ndani na kuichomekea na kisha akarukuu na Kusujudu na Shati Fupi likapanda Juu kwa ufupi au kwa kupeperushwa na Upepo basi hii hua haina Tatizo kwa sababu sehemu inayotakiwa kuhifadhiwa hua imehifadhiwa na Fulana ya ndani.

Na kwa upande wa Wanawake pia kama itakua amevaa Soksi Miguuni au kitu chochote kile kitakacho hifadhi ngozi ya Miguu isionekane na kisha akarukuu au kusujudu na Nguo ikapanda Juu au ikapeperushwa na Upepo na kuonesha miguu yake basi haitokua na Tatizo kwa sababu Miguu na Nyayo zake zimefunikwa na Soksi alizovaa juu ya Miguu yake.

SIJDA JUU YA MGONGO WA MTU NDANI YA SALA.

❖❖❖

Kwani katika wakati wa Mamlaka ya Amir ul Muuminin Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* basi katika Ijumaa Moja Umar Ibn al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alipanda kwenye Mimbar na Kutoa Khutba.

Na hivyo akaona kua Umati wa Watu Umejaa kiasi ya kua Hamna Nafasi hata ya Kusujudu vizuri bila ya kugusana kwa watu walio ndani yake, wacha Mbali waliokua nje yake.Hivyo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema:

إنَّ رسولَ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ بَنى هذا المسجدَ ونحن معه: المهاجِرونَ والأنصارُ، فإذا اشتَدَّ الزِّحامُ فلْيسجُدِ الرجلُ منكم على ظهرِ أخيه

Hakika Msikiti huu umejengwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Na sisi tulikua pamoja nae. Muhajirrin (Waislam Waliohama Kutoka Makkah kukimbilia Madina) na Ansari (Waislam Wa Mji wa Madina Waliowanusuru Waislam wa Makkah walipohamia Madina kwa kuwapokea na kuwkaribisha)

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akaendelea kusema kua: '**Hivyo Kama Watu wakiwa wengi Sana basi wacheni Miongoni mwetu wawe ni wenye Kusujudu juu ya Mgongo wa Mwenzake.'** *(Musnad Imam Ahmad)*

Kwani Hadith hii ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambayo inaruhusu kwa Waumini Kusjudu juu ya Migongo ya Wenzao pale inapokua hakuna Nafasi Ndani ya Msikiti inazungumzia kuhusiana na hali ilivyokua hapo kabla katika Wakati wa Kujengwa kwa Msikiti wa Madina na *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam.* Ambao ulijengwa kulingana na Idadi ndogo ya Waumini wa Mji huo katika wakati huo ambapo walikua ni Muhajirrina na Maansari tu.Lakini baada ya kupita mda na Mamlaka ya Utawala wa Kiislam kukua na Wafuasi kua wengi zaidi, basi hali ilibadilika kiasi ya kua Msikiti huo ukawa Mdogo kabisa.

Na hivyo akawaamrisha watu kua Kama Msikiti umekua Mdogo basi na wasujudu juu ya Migongo ya wenzao.Kwani Hadith ambayo ni Sahih hii pia imenukuliwa na ImamAl Bayhaqi katika Sunnah yake ambae nae amesema ni Hadith Sahih pia.

Ambapo anasema Imam Al Bayhaqi kua: '**Amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua, kama Msikiti utakua umejaa sana basi wacha Miongoni mwenu wasujudu juu ya Migongo ya wenzao.'**

Imam Al Bayhaqi anaendelea kusema kua: **'Hivyo Inaruhusiwa Kusujudu juu ya mgongo wa Mtu pale inapokua hna nafasi Msikitini hata bila ya kua na ruhusa kwa mwenzako huyo, na hii ni kwa sababu ya Dharura, na pia kwa sababu hakuna kisingizio cha kuachana na Kusali Sala ya Ijumaa.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi basi anasema kua:**'Kama ikiwa Msikiti umejaa sana na mwenye Kusali amekosa sehemu ya Kusjudia ardhini basi na Asujudu juu ya Mgongo wa mwenzake au juu ya Mguu wa mwenzake aliekua Mbele yake,na hio hua ni Wajibu kwake katika Kutimiza Nguzo ya Kusjudu**. **Na huu pia ndio Mtizamo wa Imam An Nawawi, Imam Abu Hanifa, Imam Al Shafii, Imam Abu Thawr na Imam Ibn Al Mundhir.'**

'Ama kuhusiana na Mtizamo wa Imam Malik, Imam Ataa na Imam Az Zuhri basi wao wanasema kua La hairuhusiki kufanya hivyo.'

Na anasema pia Shaykh Ul Islami Imam Abu Yahya Muhammad Ibn Zakarriyah Ibn Zayn Al Din Al Sunayki Al Ansari Al Shafii kua: '**Inaruhusiwa Kusujudu juu ya mgongo wa Mtu pale inapokua hamna nafasi Msikitini hata bila ya kua na ruhusa kwa mwenzako huyo, na hii ni kwa sababu ya Dharura**. **Na hivyo kama ikiwa Mtu atajiuzuia Kusjudu katika hali kama hii basi Mtu huyo hua Hana Sala, na hairuhusiki kwake yeye Kuivunja Sala hio na kuachana nayo, kwa sababu Kuacha Kusali Sala ya Ijumaa kwa Makusudi kwa Mategemeo ya kua Utaisali baadae hua hakuna sababu ya Msingi inayokubalika.'**

'Na juu ya hili wamethibitisha Maimam wawili(Yaani Imam Al Ramli na Imam An Nawawi) Ambapo kwa Upande wa Al Qadhi Al Baghawi nae amesema pia kua inaruhusika kutokana na Dharura. **Na Al Qadhi Al Baghawi amenukuu kutoka katika Maandishi ya Imam Al Shafii ambae**

aliulizwa kuhusiana na hili na akasema kua inakubalika kutokana na kuwepo kwa hali ya nadra ambayo si ya Kudumu na kuendelea'*(Asna Matalib)*

Kwani kwa maana hio Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Al Shafii, Imam Hanbal na baadhi ya Wanazuoni wa Imam Malik wanakubaliana juu ya kukubalika kwa Mtu kusujudu juu ya Miguu, au Mgongo wa mwenzake pale inapokua kuna dharura ya kukosekana nafasi ya Kusujudia kutokana na wingi wa Watu.

Na hii ni kulingana na vithibitisho vya Aya na Hadith kua Kila Mtu ajitahidiKutekeleza Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Kadri atakavyoweza.Kwani amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Kama nikikuamrisheni kufanya kitu basi kifanyeni kwa kadri mtakavyoweza na nikikukatazeni kitu basi achaneni nacho.'**

Hivyo pale inapotokea kua Mtu amejikuta katika Msikiti uliojaa sana Watu na Labda amekwama baina ya watu Ngazini au Nyuma kabisa. Ukutani Hawezi kutoka wala kuenda mbele wala nyuma na Sala inasaliwa basi kwa Mtu husika humbidi kusali na kusujudu ndani ya Sala hio kulingana na Mazingira ya hali aliyokua nayo katika wakati huo.Hususan tunapozungumzia Sala ya Ijumaa ambayo ni Sala isiyolipika fidia kwani kama ikikupita basi ndio imekupita.

SUJUD NA MANUFAA YAKE KWA AFYA YA IBN ADAM.

❖❖❖

حدثنا جعفر بن مسافر حدثنا السري بن مسكين حدثنا ذواد بن علبة عن ليث عن مجاهد عن أبي هريرة قال هجر النبي صلى الله عليه وسلم فهجرت فصليت ثم جلست فالتفت إلي النبي صلى الله عليه وسلم فقال اشكمت درد قلت نعم يا رسول الله قال قم فصل فإن في الصلاة شفاء حدثنا أبو الحسن القطان حدثنا إبراهيم بن نصر حدثنا أبو سلمة حدثنا ذواد بن علبة فذكر نحوه وقال فيه اشكمت درد يعني تشتكي بطنك بالفارسية قال أبو عبد الله حدث به رجل لأهله فاستعدوا عليه

Kwani anasema Jafar Ibn Musafir kua amesema Al Sari Ibn Maskiin, kua amesema Dhuwad Ibn Ulbah kua amesema Layth kua amesema Mujahidkua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua katika hali ya Ihram Na mimi pia nilikua katika hali ya Ihram, hivyo nikasali na kisha nikakaa kitako.**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanigeukia na kuniuliza: 'Vipi? Unaumwa na Tumbo?'**

Nami nikasema 'Naam Ya Rasul Allah!'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema, 'basi Simama Usali, kwani Katika Sala hua Mna Tiba ndani yake'*(Sunan Ibn Majah)*

Na amesema Abu Hasan Al Qattan kua amesema Ibrahim Ibn Nasir kua amesema Abu Salamah kua amesema Dhuwad Ibn Ulbah Alituambia Sisi Kitu kama hicho ambapo yeye aliuliza kwa Kiajemi kwa kusema kua Jee Unaumwa na Tumbo.'*(Sunnah Ibn Majah)*

Naam hivyo tunapoangalia kuhusiana na Sujud na Ibada ya Sala kwa Ujumla kulingana na Hadith hii basi mbali ya kua kuitekeleza kwake hua ni Kutekeleza Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambayo humpelekea kila mwenye kuitekeleza kua ni mwenye Kupata Ponyo la Kimoyo na Kinafsi na hivyo Mja husika kuingizwa ndani ya Rehma za Allah Subhanah wa Ta'ala na kunufaika na kila chenye kheri na manufaa nae kutoka kwa Mola wake na kuepushwa na kila lenye Shari nae kutokana na amrisho la Mola wake ambae ndie aliemuumba.

Hivyo Mtu anaetekeleza Jukumu la kusali Sala zake zote za kila siku na hivyo kua ni mwenye Kusujudu mbali ya kua ni mwenye kua na Ukaribu na Mola wake kama ilivyosema Hadith kua: Mja hua na Ukaribu na Mola wake pale anapokua katika Sijda hivyo ombeni Dua ndani yake. Ambapo kitendo cha Kusujud na kugusisha Ardhini Paji la Uso ndio kitendo chenye upekee katika Ibada kwani hua kinatekelezwa katika Ibada ya Sala ya Kiislam tu.

Kwani Muislam anapoingia katika Ibada ya Sala na kisha ndani yake akasujudu basi hua ni mwenye kuufanya mwili wake wote kua ni wenye kua katika mwendo, kwani Kuinama kwake Mtu na kuingia kwenye Sujud huku kichwa chake kikiwa Ardhini na Mikono yake ikiwa pembeni yake basi takriban Misuli yake yote ya Mwili hua ni katika kufanya Mazoeni ya Mwili.
Kwani mbali ya kua Katika Sujud na Sala mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua mnapatikana tiba ya Kiroho ndani yake. Lakini pia tunapoangalia kuhusiana na namna alivyoamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusujudu ndani ya Sala basi tinaona kua ameshurutisha kwa Mwanamme Mikono isibanwe mbavuni bali itanuliwe. Na hivyo kitendo hiki cha kutanua mikono hua kinazipelekea sehemu za juu ya mikono kua ni yenye kubeba Uzito wa Mwili katika Kusujudu Na hukazanisha Misuli ya sehemu hizo za Juu za Mikono.

Ambapo kwa upande mwengine basi tunapokiangalia Kichwa ambacho ndio kiungo cha mwili hua kipo chini zaidi kuliko Viungo vyengine vyote Vyenye kubeba Mifumo Muhimu ya Ufanyajikazi wa Mwili, ambapo Mfumo Mkuu wa ufanyaji kazi ndani ya Mwili hua ni Moyo kisha unafuatia Ubongo. Ambao unakaa kichwani, Na kisha ndio inafuatia Mifumo myengineyo ya Mwilini.

Na mara zote katika Harakati zetu za kimaisha basi Ubongo hua Uko Juu zaidi kuliko Moyo, kwani na hii ni kwa sababu Kichwa hua ni sehemu ikaayo Juu kwenye Mwili. Lakini Mtu unapoingia kwenye Ibada ya Sala na kisha Ukasujudu ndani yake basi Kichwa hua chini zaidi kuliko Moyo.

Jambo ambalo hupelekea Mfumo wa Mzunguko wa Damu kua ni wenye kutiririkia zaidi Kichwani. Na hii kuupelekea Ubongo Kunawirika zaidi Kiufaham, Kikumbukumbu, na Kihisia za Kuona na kusikia kutokana Kutiririka kwa Wingi wa Damu ndani yake katika Wakati wa Kusujudu.

Na ndio maana Watu wanaosali hua ni wenye Kua na Uwezo Mkubwa wa Kustahmili na kua na Subra na Mitihani pale inapowafika kuliko wale Wasiosali. Na hunufaika kutokana na kutoumwa na Maradhi tofauti yanayotokana na Ufahamu na Ubongo kama Kuchangangikiwa, Kupatwa na Msongo wa Mawazo n.k

Na si Kichwa na Ubongo na Mikono tu inayonufaika kutokana na kitendo cha Kusujudu, bali pia na Mishipa ya Shingo, hunufaika kwa Kua ni yenye kufanyishwa mazoezi ya Kukakamaa na kuimarikaKwani Katika Kusujudu basi Mishipa na Misuli ya sehemu za shingoni.

Hua ni yenye Kukaza kutokana na kukisimamia Kiungo hicho Kukipa nguvu Kichwa kustahamilia Kuubeba Uzito wa Mwili Mzima wa Ibn Adam alieingia katika Hatua hio ha Kusujudu mbele ya Mola wake.Na mtu unaweza kuhisi Uzito huo pale unapokua umebakia katika hatua hio ya Sijda kwa Mda mrefu kidogo katika kufanya Dhikr au kuomba Dua kwako.

Na pale unaponyanyua Kichwa chako kutoka kwenye Sijda hata kama ulikua hukukaa kwa mda mrefu kwenye Sijda basi hua ni mwenye kuhisi namna Misuli ya Shingo na Uso inavyojivuta kutokana na kuubeba Uzito wa Mwili na kuurudisha katika hali ya kukaa au kusimama kwa kawaida.Ambapo kukakaza huko kwa Misuli hio hua ni sehemu ya Kuimarisha Uti wa Mgongo pia.

Kutoka kichwani, kupitia shingoni hafi mgongoni na kiunoni.Hivyo miongoni mwa manufaa ya Sujud za Ndani ya Sala katika Kuinama na kuinuka basi pia hua ni Kuimarisha Misuli ya Mgongo na Kiuno.
Na bila ya shaka kuendelea Kufanya Sijda katika Rakaa ya Sala mara tano kwa siku ambamo ndani yake hua mna Sijda 34 hua ni Zoezi tosha la Kuimarisha viungo hivyo kama ilivyoamrishwa na Muumba aliemuumba Kiumbe bora na mwenye *Taqwim* bora zaid ambae ni Ibn Adam.

Ibada ya Sala pamoja na Sujud ndani yake hua pia ni yenye Kuimarisha Mfuko wa Uzazi wa Mwanammke.Hususan kwa Wanawake wenye Matatizo ya Kupindia kwa Nyuma sehemu ya Shingo ya Kizazi chao kwani katika Kusujudu kwao basi eneo hilo hua ni lenye Kulazimika Kukaa Sawia kutokana Kusumwa kutoka katika Muelemeo wa nyuma na kuelekea katika Muelemeo wa mbele.

Na bila ya shaka Kusujud hua ni sehemu ya Mazoezi ya Kuongeza Nguvu za Kiume.Kwani katika Kusjudu na Kunyanyuka na Kuja Juu basi Misuli ya Sehemu za Siri hua ni yenye kujikaza na Kujivuta ambalo hili pia hua ni zoezi tosha la kuondoa Matatizo ya Upungufu wa Nguvu za Kiume.Hivyo kila mmoja inabidi ajiulize kua Jee anasujudu ipasavyo?. Kwani ni pale utakaposujudu ipasavyo tu basi ndio atakaponufaika na Faida za Sijda kwa Afya yako.

Ambapo tunaporudi kwa Upande wa kichwa na Paji la Uso na Ncha ya Pua kushurutishwa Kugusa Ardhini kama alivyoamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi tunaona kua Unapoweka Paji lako la Uso ardhini basi kimaumbile Paji lako la Uso na Pua hua ni vyenye Kuchota au kunasa sehemu za electrons huru ambazo huhitajika katika Kuimarisha Miili ya Ibn Adam kwa kupunguza wingi wa vyanzo vya Tishu za Mwilini zisizohitajika ambazo kama zikibakia kwa wingi basi huweza kusababisha Maradhi mbali mbali ikiwemo Saratani.

Hivyo haishangazi kuona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaambia Masahaba zake Radhi Allahu Anhum kua Wasujudu Chini Ardhini, yaani aasisujudu juu ya Kitu kama tulivyoona hapo kabla katika Hadith.Na hii ni kwa sababu unaposujudu juu ya Zulia, Jamvi, Msala na Juu ya Nguo na Unaposujudu Juu ya Mchanga, Saruji au Tiles hua kuna Utofauti wa Unasaji wa Electrons husika.

Yaani tuchukulie Mfano wa Paji la uso kua ni Sumaku na Ardhi kua Ni yenye kumwagiwa Unga wa Chuma. Hivyo ukigusisha Sumaki moja kwa moja juu ya Ardhi badi Utanasa unga wa Chuma zaidi kuliko ukaweka Zulia juu ya Ardhi yenye Unga wa chuma na kisha Ukaweka Sumaku Juu yake.

Na Kimaumbile katika mazingira yetu hua pia tumezungukwa na Mawimbi mbali mbali ya Nguvu Umeme Sumaku yenye Madhara ambayo yanatuathiri sana Miilini mwetu ikiwemo Mawimbi ya Mionzi ya Radio, Tv, Simu, ya Mitandao, Wifi n.k. Na njia pekee ya Kujisafisha kutokana na Athari za Mionzi hio hua ni Kugusiha Paji la Uso Ardhini, kwani kufanya hvyo hua ni Kupunguza na kuua Nguvu za athari hizo kutoka ndani ya Miili yetu. Hivyo Kusujudu Juu ya Ardhi huonda Chaji Hasi ya Nishati

yenye Kupelekea kua na Athari Mbovu ndani ya Miili yetu. Chaji Hasi husababisha Hasira za Ovyo, Chuki, Wivu, Husda, Msongo wa Mawazo n.k

Kwani Mwili wa Ibn Adam una vyanzo vya Tishu zifikazo *Quintillion* 7 yaani Bilioni 7 mara 7 mara 7 7000, 000,000,000,000,000,000,000,000. Hivyo wingi wake huu unapozidi basi husababisha Madhara ya Saratani, na unapopungua pia husababisha madhara kwani hupelekea sehemu za mwili husika kuanza kuharibika na kuoza.Na katika mazingira tunayoishi basi uwezekano wa kuongezeka hua ni mkubwa kuliko wa kupungua kiidadi.

Hivyo njia pekee ya Kuhifadhi afya zetu kutokana na Athari za Chaji hasi zinazotuzunguka ni Kusjudu kwa Wingi na kwa mda mrefu ndani ya Sala zetu.Kwani Ndani ya Sala Mna Tiba

JALASAH AL ISTIRAAHA KIKAO BAADA YA SIJDA YA PILI

❖❖❖

Baada ya kumalizana na hatua ya Sujud zote mbili za Rakaa za SalaNa hivyo tunaingia katika Kitendo kinachofuatia baada ya kutoka katika Kusuju Sijda ya Pili ya Rakaa ndani ya Sala.Ambapo kitendo hicho kinachofuatia Ndani ya Sala kinaitwa *Al Jalasa Al Istraaha* na kuelezewa kama ifuatavyo:

جلسة الاستراحة: هي جلسة خفيفة يجلسها المصلي بعد الفراغ من السجدة الثانية من الركعة الأولى قبل النهوض إلى الركعة الثانية وبعد الفراغ من السجدة الثانية من الركعة الثالثة قبل النهوض إلى الركعة الرابعة.

Jalasa Al Istraaha maana yake hua ni Kikao cha Kukaa Kitako kwa mda Mfupi ambacho hua kinatekelezwa mara tu baada ya Sijda ya Pili katika Rakaa za Witri za Sala yaani Rakaa ya kwanza ya Sala ya Rakaa Mbili, na pia mara tu baada ya Sijda ya Pili Katika Sala ya Kwanza na ya Tatu katika Sala ya Rakka Nne kabla ya Kusimama kwa Ajili ya Kisimamo cha Rakaa zinazofuatia, iwe katika Sala ya Fardhi ama Sala ya Sunna.

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: '***Jalasa Al Istiraaha,* hua ni Kikao Kifupi kinachofuatia baada ya Sujud ya Pili na Kabla ya Kusimamo katika Kisimamo cha Sala**. **Na Kufanya hivyo *(Jalasa Al Istiraaha)* hua ni Sunna kulingana na Mtizamo wa Imam Al Shafii, Imam Is-haq Ibn Rahawayh na Imam Ahmad Ibn Hanbal.**

Na hii ni kutokana na Hadith ya Abu Qilabah Abdullah bin Zaid Al Jarmi Al Basri,ambae amesema kua: Malik Ibn Huwayrih alitusalia sisi Sala ya *Rasul Allah Salallahu Allahu Alayhi wa Salam* na hivyo pale aliponyanyua Kichwa chake kutoka katika Sijda ya Pili ya Rakaa ya Kwanza, alikua ni mwenye Kukaa Kitako Kidogo na kisha Kunyanyuka.Hadith hii imenukuliwa na Maimam watano Isipokua Imam Muslim Ambapo maneno yaliyomo katika Hadith ya Imam Al Bukhari yanasema kua: Na pale*(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam)* anaponyanyua Kichwa Chake kutoka katika Sijda ya Pili alikua akikaa Kitako chini na kisha Husimama.

Hivyo Mimi (Imam An Nawawi) nnasema kua:Miongoni mwa Sunna hua ni *Jalasah Al Istiraaha* ambayo inatekelezwa kila baada ya Sujudu ya Pili kabla ya Kusimama.Hivyo hua haipendekezwi

kwa Mtu anaesujudu kutokana na Sijda ya Kisomo,na wala haipendekezwi kwa Mtu anaesali huku akiwa amekaa Kitako, na wala katika Rakaa ya Nne ya Sala yenye Rakaa nne na Wala katika Rakaa ambayo ndani yake mna kisomo cha *Attahiyat.*

Na ingawa inaruhusika kwa Mtu kutotekeleza lakini hua inapendekezwa, na hii ni kwa Sababu *Jalasa Al Istiraaha* hua ni bainisho la kutofautisha tofauti baina ya Rakaa mbili, na hii ni Kulingana na Mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab (ya Imam Al Shafii).Na hua ni Bora kwa *Jalasa Al Istiraaha* kua isiwe ni yenye kuzidi urefu wa mda wa kupata Utulivu katika Kukaa, na hii ni kwa sababu kufanya hivyo hua ni Sunna tu'*(Al Fatawa An Nawawi)***

Naam tumeanza kuelezea Kuhusiana na Jalasa Al Istiraaha kulingana na Mtizamo wa Madhhab Imam Al Shafii kulingana na Fatwa ya Imam An Nawawi.Hivyo ili kufahamiana zaid basi inabidi na tuangalie Mitizamo ya Madhhab mengine na Wanazuoni wengine kuhusiana na Kikao hiki, kwani iuna Mtizamo tofauti juu yake.Ambapo tunapoangalia kwa kina basi tunaona kua Kwanza Wanazuoni wanakubaliana kua *Jalasa Al Istiraaha* hua Si Lazima, na wala Si Wajibu bali ni Sunna.

Na kwa kua kuna Makubaliano hayo ya kua sio Wajibu wala sio lazima kukaa kikao hicho bali ni Sunnah basi kuna mitizamo Mitatu tofauti Juu yake. Ambapo Mtizamo wa Kwanza ni Kua Haipendekezwi kukaa *Jalasat Al Istiraaha* kama ikiwa hakuna haja au sababu ya kufanya hivyo na huu ni Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Mitizamo ya Masahaba na Wanazuoni wa Tabiina yaani Vizazi vilivyofuatia baada yao.

Ambapo Miogoni mwa Masahaba wenye Mtizamo huu ni Pamoja na *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,Amir Ul Muuminin* Ali Ibn Abi Talib *Karamah Allahu Wajh,* Abd Allah Ibn Masid *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu.*

Na Miongoni mwa Maimam wenye Mtizamo huu ni pamoja na Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Abu Hanifa Nuuman Ibn Thabit, Imam Malik Ibn Anas, Imam Abu Al Ziyad, na imenukuliwa pia mara moja kutoka kwa Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Is-haq Ibn Rahawayh na mara mbili kutoka kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal. Kama ilivyoainishwa kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa katika kitabu *Al Bina'ah* cha Imam Al Ayni.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik katika Al Majmaa Al Anhar cha Imam Zadeh, Na Hashiyat Al Adwi ala Kifayat Al Talib cha Imam Al Rabbani. Al Fawaqi Al Dawani cha Imam Al Nafrawi. Na kama alivyosema Imam Ibn Rushd katika *Bidayat Al Mujtahid,* kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Al Buhuti katika *Kashf Al Qina* na Al Mughni ya Imam Ibn Qudamah.

Ambapo kwa upande wa Imam Al Shafii ni kama alivyosema Imam An Nawawi pia katika *Rawdah At Talibin.*

Na anasema Imam Ibn Al Qayyim kua:**'Kulingana na Hadith basi bila ya shaka kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikaa *Jalasa Al Istiraaha* kwa ajili ya Kupumzika, lakini hakukaa kwa ajili ya kua kufanya hivyo kua ni Sunna miongoni mwa Sunna za Sala kama Kufunga na kuachia Mikono n.k. Hivyo huenda kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifanya hivyo kwa sababu alihitajia kufanya hivyo kutokana na Utu uzima labda.'**

Na kwa Wanazuoni wenye Mtizamo huu aliouelezea Imam Ibn Al Qayyim hua ni wenye kusimamia katika Hoja zfuatazo:

Kwanza ni kutokana na Hadith ya Wail Ibn Hujayr na Abu Hurayrah ambazo tumeshaziangalia mara kadhaa katika mada yetu hii ambazo zinaonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuwa akikaa kikao baada ya Sijda mbili za Rakaa za witri za Sala yaani Rakaa ya kwanza na ya Tatu.

Pili ni kutokana na Masahaba *Radhi Allahu Anhum* ambao walikua wakimfuatilia Sana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala zake ambao nao pia walikua hawakai kikao hiki katika Sala zao.

Kwani Kulingana na Vithibitisho hivyo basi Wanazuoni wenye Mtizamo huu wanasema kua**: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akikaa Kikao hiki katika wakati ambao alikua Akiumwa, kwa mfano kama inavyoelezewa katika Hadith ifuatayo katika Sahih Muslim ya Abd Allah Ibn Shaqiq ambae alimuuliza Ummu ul Muuminina Aisha *Radhi Allahu Anha* baada ya kusema:**

عن عائشة – رضي الله عنها – قالت: «لَمَّا بدَّن رسولُ الله صلَّى اللهُ عليه وسلَّم وثقُل كان أكثر صلاته جالسًا»، وسألها عبد الله بن شقيق: هل كان النبي صلَّى اللهُ عليه وسلَّم يُصلِّي وهو قاعد؟ قالت: «نعم، بعدَما حَطَمَه النَّاسُ

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliponenepa alikua akisali takriban Sala zake zote huku akiwa amekaa Kitako.Hivyo Abd Allah Ibn Shaqiq akauliza*: Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali huku akiwa amekaa Kitako?**

Ummu ul Muuminin* Aisha*Radhi Allahu Anha* akasema: 'Naam baada ya Kuumizwa na Watu.'(Sahih Muslim)***

Na kwa upande mwengine basi kuna Hadith ya *Ummu ul Muuminin* Hafsah Bint Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua:

ما رأيت النبيَّ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم يصلِّي في سبحته قاعدًا، حتى كان قبل وفاته بعام فكان يصلِّي في سبحته قاعدًا

'Sikuwahi mimi kumuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisali huku akiwa amekaa Kitako hadi katika mwaka wa Mwisho wa Uhai wake, alikua akisali huku akiwa amekaa Kitako'*(Sahih Muslim)*

Na pia kuna Hadith kutoka kwa Muawwiyah Ibn Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu* ambayo amesema kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituambia sisi kua: 'Msiniharakishe katika Kurukuu na Kusujudu kwani nimekua ni mwenye kuzidi Uzito'*(Sunan Abu Daud,Sunan Ibn Majah, Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal)***

Ambapo anasema Imam Ibn Rajab Al Hanbal kuhusiana na vithibitisho hivi kua: '**Takriban Hadith zote zilizokua zikielezea Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hazikuelezea kuhusiana na Jalasat Istiraaha kikao cha Kupumzika baada ya Sijda mbili, hivyo kama ingekua ni Sunnah basi bila ya shaka ingeelezewa**. **Ambapo jambo hili linathibitisha kua Kukaa *kwake Rasul Allah***

Salallahu Alayhi wa Salam **katika** ***Jalasat Al Istiraaha*** **ilikua ni kutokana na Hali ya Dharurah aliyokua nayo.'***(Fat-h Al Barr Imam Ibn Rajab Al Hanbal)*

Hivyo huo ni Mtzamo wa kwanza kuhusiana na *Jalasa Al Istiraaha* hivyo baada ya kuona Mtizamo huo basi na tuangalie Mtizamo wa pili ambao ni wa Wanazuoni wenye kusema kua: **'*Jalasa Al Istiraaha* yaani Kukaa Kitako kidogo baada ya Sijda ya pili za Rakaa za Witri Sala yaani baada ya Rakaa ya Kwanza na baada ya Rakaa ya Tatu hua ni Sunna inayopendekezwa'**

Ambapo huu ni Mtizamo wa miongoni mwa Masahaba akiwemo Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu*, Malik Ibn Huwayrih *Radhi Allahu Anhu* na Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu.*Na miongoni mwa Maimam wa Tabiina ni pamoja na Imam Abu Qilabah Abdullah bin Zaid Al Jarmi Al Basri.

Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ni kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi katika *Al Fatawa* basi na ndio hivyo hivyo alivyosema katika Al Majmuu kua: '***Jalasa Al Istiraaha*** **hua ni Sunna Inayopendekezwa, hivyo yeyote yule atakaetoka kwenye Sujud kwa ajili ya Kisimamo cha Rakaa ya Pili au kwa ajili ya Kisimamo cha Rakaa ya Nne, basi hua inapendekezwa kua asisimame moja kwa moja bali akaekitako kidogo hadi mgongo ukae sawia na kisha ndio anyanyuke kwa ajili ya Kisimamo, na huu ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.'***(Al Majmuu)*

Kwani Mtizamo huu pia umeungwa mkono kwenye kitabu cha Imam Sulayman Ibn Umar Al Jamal Al Ajli Al Shafii kiitwacho *Hashiyat Al Jamal aAla Sharh Al Minhaj.*Na pia na Imam Al Buhuti Al Hanbali katika *Kashf Al Qinaa,* Na pia katika *Fat-h Al Barr* ya *Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami* Ibn Hajar Al Asqalani Al Shafii.

Na Wanazuoni wengineo wakiwemo Wafuasi wa Madhhab ya Imam Daud Ad Dhahiri Na pia Imam Al Shawqani Al Hanbali ambae yeye amesema katika kitabu chake cha Nayl Al Awtar kua: '**Hadith inazungumzia kuhusiana na kuruhusika kwa *Jalasat Al Istiraaha* baada ya kumaliza Sujud ya pili na kabla ya kunyanyukwa kwa ajili ya Kisimamo cha Rakaa ya Pili na ya nne, na Imam Al Shafii alifuata Mtizamo huu unaojulikana sana kutoka kwake na kutoka kwa baadhi ya Wanazuoni wa Hadith,na kutoka kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal kuna Nukuu mbili juu ya Jambo hili'** *(Nayl Al Awtar)*

Hapa katika kuelezea kwao Maimam kuhusiana na Mitizamo hii basi tumeona kua kuna wanaosema kuhusiana na kua Mtizamo wa Kutopendekezwa kukaa *Jalasat Al Istiraaha* kua kuna mtizamo mmoja kutoka kwa Imam Al Shafii,na Miwili kutoka kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal na kwa Imam Is-haq Ibn Rahawayh.

Na hapo hapo kuna wanaosema kua Mtizamo wa kua inapendekezwa kukaa *Jalasat Al Istiraaha.* Pia ni kutoka kwa Imam Al Shafii kama alivyosema Imam Al Shawkani katika Nayl Al Awtar na kua pia Imam Al Buhuti amesema kua huu pia ndio Mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Kwa hivyo tukiaangalia hapa hua tunaona kua kama kuna kupingana baina yao Maimam hawa kua mara inapendekezwa mara haipendekezwi.Hivyo kwanza ili tufahamu na kuondoa kasoro hii basi inabidi tukumbuke kua Maimam hawa wote watatu waliishi kipindi kimoja.

Kama tulivyosema hapo awali kua walikua ni Mwalimu na wanafunzi wake yaani Imam Al Shafii alikua Mwalimu wa Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Is-haq Ibn Rahawayh.Na hiki kilikua ni kipindi ambacho Imam Al Shafii alipokua akiishi Mjini Baghdad.

Ambapo tumeona hapo awali kua hawa wote ni Maimam Wakubwa sana Kiilm, na katika Kusoma kwao basi kila mmoja wao alikua na Mitizamo yake.Ambapo baadhi ya Wakati katika Kusomeshwa kwao basi Mitizamo ya Imam A ShafiiIlikua ikipingana na Mitizamo ya Imam Is-haq Ibn Rahawayh.Lakini baada ya kuhojiana na kufahamishwa na Imam Al Shafii kuhusiana na Mitizamo husika Imam Ibn Rahawayh alikua akibadilisha Mitizamo yake na kuamua kufuata Mitizamo ya Imam Al Shafii kutokana na Nguvu za vithibitisho vya Imam Al Shafii.

Ambapo kwa upande wa Imam Ahamd Ibn Hanbal basi yeye alikua akichanganya Mitizamo kulinganana Ufahamu wake juu ya jambo husika na hivyo alikua akitumia Mitizamo yake, Mitizamo ya Imam Al Shafii na Mitizamo ya Imam Ibn Rahawayh hata kama Ibn Rahawayh ameachana na Mtizamo huo kutokana na Nguvu za Vithibitisho vya Mtizamo wa Imam Al Shafii wakati Imam Hanbal akiwa pamoja nao katika Majadiliano ya jambo husika.

Na baada ya mda Imam Al Shafii akahama katika Mji wa Baghdad na kuhakia Misri kwa ajili ya kumfuata Imam Saad Ibn Al Layth ili asome kwake.Na Imam Ibn Rahawayh nae akahama Baghdad na kuelekea Khurasan, na hivyo Baghdad akabakia Imam Hanbal peke yake. Na baada ya Imam Al Shafii kuhama Baghdad basi alisema kua: '**Hakika mimi sikuwacha Mtu mwenye Ilm Mjini Baghdad kama Ahmad Ibn Hanbal na sikuwacha Mtu mwenye Ilm katika Ardhi ya Khurasan kama Ibn Rahawayh.**'

Hivyo kusikia Wanazuoni wakiwa Wanawahusisha Maimam hawa watatu pamoja katika Jambo moja wakiwa na Mitizamo tofauti ndani yake hua si jambo la kushangaza sana. Kwani Maimam hawa Maisha yao yote walikua wakisoma hivyo kuna wakati inatokea Imam husika kua na Kauli mbili Juu ya Jambo husika yaani kwanza labda alikubali kua ni Suna kisha baadae akakataa kua si Sunna.Na hii ni kwa sababu katika kusoma kwao Walikua kila wanapopata Uthibitisho wenye Nguvu zaidi labda kutoka katika Aya au Hadith,nk basi Mtizamo usiokua na nguvu ya hoja hua wanauacha.

Na ndio maana tunaona kua hata Imam Al Shafii mwenyewe alikua akisema kua Fatwa zake anazotaka zifuatwe ni zile zilizomo kwenye Kitabu cha Al Umm ambacho alikiandika Alipokua Misri, baafa ya Kuondoka Baghdad mbali ya kua alikua tayari ameshatoa kitabu cha Al Risala kabla ya kuenda Baghdad.Na hata Imam Ahmad Ibn Hanbal nae pia alipoulizwa kuhusiana na Vitabu viwili vya Imam Al Shafii yaani Kitabu cha Al Risala alichokiandika wakati akiwa Mjini Makkah mwanzoni mwa Uimam wake na Kitabu cha Al Umm alichokiandika miwishoni mwa Uhai wake.

Basi Imam Ahmad Ibn Hanbal alisema: '**Nukuuni kutoka katika Al Umm, na Msinukuu kutoka katika Al Risala.**'

Na hali hii haipo kwa Maimam hawa tu, bali pia ipo kwa Maimam wengineo, kwa mfano Wanafunzi wa Imam Abu Hanifa ambao ni Imam Abu Yusuf na Imam Ash Shaybani.Nao pia kuna Fatwa ambazo walikua wana mitizamo miwili, ambapo Mtizamo mmoja ni kutoka kwa Mwalimu wao Imam Abu Hanifa kabla ya Al Shaybani na Abu Yusuf kukutana na Imam Al Shafii.Na hivyo Baadhi ya Mitizamo waliibadilisha na kuamua kuachana na Mitizamo ya Mwalimu wao Imam Abu Hanifa baada ya kukutana na Imam Al Shafii na kujadiliana nae juu ya mambo husika na wakaamua kufuata Mitizamo ya Imam Al Shafii.

Na labda tutoe mfano mmoja ambao unawachanya sana Wasiotaka kujua ambao ni Mtizamo wa Muandamo wa mwezi mmoja kwa Dunia nzima.Ambapo Fatwa hio ni ya Imam Abu Hanifa na kina Abu Yusuf na Imam Ash Shaybani walikua wakikubaliana na Fatwa hio,lakini baada ya kujadiliana na Imam Al Shafii basi wakaamua kufuata Mtizamo wa Imam Al Shafii kua kila sehemu na Muandamo wake baada ya wao kuthibitishiwa na kuridhika na vitihibitisho vya Imam Al Shafii.

Na ndio Maana utasikia kua Katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua kuna Mitizamo miwili juu ya Fatwa hio.Ambapo Moja ni ya Imam Abu Hanifa na ya Pili ni ya Wanafunzi wa Madhhab yake, kutokana na Mtizamo wa Imam Al Shafii.Na kutokana na kua Mtizamo huu ndio wenye Vithibitisho vyenye nguvu Ki Aya, Kihadithi, kihoja na kiakili na pia ndio mtizamo wa wengi basi ndio ukawa Mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Hii ni miongoni mwa sababu za Maimam kua na baadhi ya Mitizamo inayotofautiana katika Jambo fulani, na hivyo tunarudi katika Mada yetu ya *Jalasat Al Istiraaha*ambayo ndani yake tunaona kuhusiana na Mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal kama unavyoelezewa na Imam Ali Ibn Sulayman Al Mardawi Al Hanbali katika kitabu chake cha Al Insaaf ambacho kinasema:

‘**Imenukuliwa kutoka kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal kua Mtu anaesali anatakiwa akae katika Jalasat Al Istraaha; ambapo huu ndio mtizamo pia uliopendekezwa na kukubalika na Imam Abu Bakr Ibn Aziz na Ahmad Ibn Muhammad Al Baghdadi Al Khallaal Al Hanbali, ambae amesema kua Imam Ahmad Ibn Hanbal aliufuta Mtizamo wake wa Mwanzo na akasisitizia juu ya Mtizamo wake wa pili wa wa kua kukaa Jalasat Al Istiraaha kunapendekezwa.’***(Al Insaaf)***

Kwani Mtizamo huu wa kupendekezwa kukaa *Jalasat Al Istiraaha* umetajwa na kupendekezwa pia katika vitabu vyengine vya fiqh vya Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ikiwemo katika Kitabu cha *Al Riyaatayn* na *Al Hawi Al Saghir*.Ambapo Mitizamo yote miwili pia ya kuunga *mkono Jalasat Al Istraaha* na Kupinga imetajwa pia katika *Al Hidaaya, Al Mudhhab, Al Talkhis, Sharh Al Majd* na pia katika Masbuq Al Dhahab.

Na kwa upande wa Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye amesema kuhusiana na Mtizamo Jalsat Al Istiraaha kua:**‘Mtu anaekaa Jalsat Al Istiraaha hua ni yule ambae ni dhaifu na Mgonjwa.’**

Kwani tunaporudi kwa Imam Abu Bakr Al Khallal Al Hanbali basi yeye anaendelea kusema kua:**‘Amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi* alikua akikaa *Jalasat Al Istikhara* kwa kukaa makalio yake, na haihesabiki mara ngapi alikua akikaa hivyo’**

Na pia Imam Ahmad Ibn Hanbal amenukuliwa akisema kama alivyokua akisema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: **‘Mkao unaopendekezwa kukaa ni Mkao Ambao Mtu anakaa katika wakati anapokaa baina ya Sijda Mbili kama alivyosema Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* kua Kisha baada ya Sijda ya pili *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* alikua akikaa Kitako huku akiwa amekunja Miguu yake na kunyooka hadi pale Viungo vyake vinaponyooka na kurudi katika sehemu zake na kisha ndio Hunanyuka.’**

Na kwa upande wa Al Qadhi Al Imam Abu Yaala Muhammad Ibn Al Husayn Ibn Farrah Al Hanbali basi yeye anasema kua: **‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akikaa katika Jalasat Al Istiraaaha kwa mikao yote miwili, alikua akikalia Miguu yake na baadhi ya wakati akiweka chini Ardhini makalio yake.’**

Hivyo katika Kikao cha *Jalasat Al Istiraaha* basi Hua hamna Hamna Dhikri inayofanywa ndani yake na hii ni kwa sababu kikao hiki ambacho ni Sunna hua kinatakiwa kifanywe kwa muda mfupi kwa kadri itakavyowezekana.Hivyo kikao bora cha *Jalasat Al Istiraaha* hua ni kile kikao cha sekunde chache tu.Na Wanazuoni hua Wanapendekeza zaid kukalia mguu wa Kushoto katika kikao hiki.

Kwani anasema Imam Abu Qilabah Abdullah Ibn Zaid Al Jarmi Al Basri, ambae ni miongoni mwa Maimam wa Tabiina aliesomeshwa na Masahaba akiwemo Malik Ibn Huwayrih *Radhi Allahu Anhu* kua:**'Malik Ibn Huwayrih alikuja kwetu sisi na akatuongoza katika Sala na akasema: Mimi nnasali pamoja Nanyi, lakini Sitaki Kusali bali nnataka kukuonesheni vile ambavyo nilivyomuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyokua Akisali.'**

Ambapo Abu Qilabah Abdullah bin Zaid Al Jarmi Al Basriakaulizwa na Ayoub: **'Jee Sala yake ilikuaje?'**

Abu Qilabah Abdullah bin Zaid Al Jarmi Al Basri, akajibu: **'Kama Shaykh wetu Amr Ibn Salamah.'**

Ayoub aliemuuliza Abu Qilabah Abdullah Ibn Zaid Al Jarmi Al Basri, akasema**: 'Yaani Shaykh wetu hukamilisha Takbir na kisha anapotoka kwenye Sijda ya pili na kunyanyua kichwa basi Hukaa Kitako, kisha anajishikiza na Ardhi na Kunyanyuka kuja juu.'**

Ambapo hii kauli ya Malik Ibn Huwayrih *Radhi Allahu Anhu*haimaanishi kua alikua hataki kusali na hivyo kua ni mwenyekukataa kufanya Ibada hio, bali inaamaanisha kua alikua anataka kuainisha sababu inayompelekea Kusali, ambayo inatokana na nia ya kufundisha na hii ni kwa sababu kufundisha kwa njia ya vitendo hua kunathari kubwa zaidi uliko kwa maneno hususan tunapozungumzia jambo muhimu kama hili la Ibadaya Sala, na nndio maana hata *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* akasema: **'Salini kama mlivyoniona mimi nikisali'.** Na kwa upande mwengine pia hii inamaanisha kua Malik Ibn Huwayrih Radhi Allahu Anhu alifanya hivi katika wakati ambao si wa Sala.

Na hivyo Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kusisitiza tena kuhusiana na Jalsat Al Istiraaha kua: **'Mtizamo wetu juu ya *Jalsat Al Istiraaha* ni kua Inapendekezwa 'Kama ilivyosema hapo kabla na Malik Ibn Huwayrih *Radhi Allahu Anhu,* Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu,* Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu* na Masahaba wengineo.'**

'Na Abu Qilabah Abd Allah Ibn Zaid Al Jarmi Al Basri, pia na Tabiina wengineo, ambapo Imam Al Tirmidhii amesema kua: As-hab wetu wamesema hivyo hivyo, na Wafuasi wa Madhhab ya Dhahiri na Kauli moja ya Imam Ahmad Ibn Hanbal pia.'

Hivyo huo ni Mtizamo wa pili kuhusiana na *Jalasat Al Istraaha* hivyo tunapoangalia Mtizamo wa Tatu basi tunaona kua Kuna Wanazuoni wasemao kua:**'Inapendekezwa Kukaa *Jalasat Al Istiraaha* kwa wale watu ambao hua wanahitaji Kupumzika kidogo kutokana na Udhaifu wa Afya zao, Na hivyo basi hua haikubaliki Kukaa *Jalasat Al Istiraaha* kwa Mtu Mwenye Nguvu zake.'**

Ambapo wenye Mtizamo huuhua ni wenye Kutumia Kithibitishi cha Imam Nuuman Ibn Ayyash ambae amesema kua: **'Mimi nimewaona Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* zaidi ya Mmoja ambao walikua hawakai *Jalasat Al Istiraaha.*'** *(Imam At Tirmidhii)*

Kwani kuna Masuali kuhusiana na Jalasat Al Istiraaha ambayo Mtu anaesali Sala ya Jamaa na kisha yeye akawa ni Maamuma ambapo Suali la Kwanza ni: **'Kama Imam hakukaa Jalasat Al Istraaha baada ya Kusujudu kwa sababu kwake yeye haina haja, lakini Maamuma yeye akakaa kisha akanyanyuka, Jee Hukmu yake inakuaje?'**

Na Suali la pili ni:

‘Kama Imam amekaa Jalasat Al Istiraaha kwa Sababu kwa Mtizamo wake yeye ni kua Inapendekezwa, lakini Maamuma Hakukaa kwa sababu anaona kwake yeye haina haja, Jee Hukmu yake inakuaje?’

Naam..ama kuhusiana na hali hizi basi Wanazuoni wametofautiana juu yake, Na kutofautiana kwao kunatokana na Suali lifuatalo **: ‘Hivi Jee Kukaa Kitako kwa Maamuma kutampelekea Kuchelewa Katika Hatua za Kumfuata Imam na hivyo kua ni mwenye kupingana Na Sunna *ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ama la?’**

Kwani kuhusiana na Hali ya kwanza ambayo Imam hakukaa lakini Maamuma akaamua kukaa, basi baadhi ya Wanazuoni wanasema kua: **‘Maamuma anaweza Kukaa Jalasat Al Istraaha hata kama Imam Hakukaa, na kwa kua Kikao ni Kifupi, basi Kukaa huko hakutomchelewasha Maamuma katika Hatua za Sala na hivyo hakutosababisha Madhara.’**

Ama kuhusiana na hali ya pili ambayo Imam Amekaa kwani kwake inapendekezwa lakini Maamuma hakukaa kwa sababu kwake haina haja, basi Wanazuoni wanasema kua: ‘**Katika Hali kama hii basi hua ni Haram kwa Maamuma Kutokaa na hivyo kua ni mwenye kumtangulia Imam katika Kisimamo, hivyo hua ni bora kwa Maamuma nae kumfuata Imam katika Kukaa ili asimtangulie Imam katika Hatua za ndani ya Sala.’**

‘Na hii ni kwa Sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

انما جعلالامامليوتمبهفلاتختلفواعليهفاذكبرفكبرواولاتكبرواحتيكبرواذركعفاركعواولاتركعواحتيركعواذافلسمعا

للهلمنحمدفقولواربناولكالحمدواذاسجدفاسجدواولاتسجدواحتيسجدواذاصلىجالسافصلواجلوساأجمع

ون

Tafsir: **Imam Amechaguliwa kwa ajili ya kufuatwa, hivyo msipingane nae, atakapofanya Takbir basi nanyi Fanyeni Takbir, Na Msifanye Takbir hadi Atakapofanya yeye Takbir, Atakaporukuu basi nanyi Rukuuni, wala Msirukuu Hadi Atakaporukuu yeye, Atakaposema *Sami Allahu Liman Hamida*, basi Nyinyi semeni *Rabbana wa Laka Al Hamd,* Atakapo Sujudu basi nanyi Sujuduni wala Msisujudu Hadi Atakaposjudu yeye na Akisali akiwa amekaa basi nanyi kaeni** *(Bukhari Na Muslim)*

‘Amesema kua Imam hua amechaguliwa kwa ajili ya Kuongoza na Kufuatwa hivyo haitakiwi kupingana nae’ *(Bukhari na Muslim)*

Kwa maana hio basi Kama Imam atakua ni mwenye Kukaa Jalasat Al Istiraaha basi na Maamuma humbidi nae kukaa hata kama kwake yeye kulingana na Mtizamo wake au wa Madhhab yake kufanya hivyo hua Haina haja.Na hivyo kwa Maamuma Kumfuata Imam katika kikao hicho hua ni kutekeleza Sunna ya Kikao hicho na pia Sunna ya Kumfuata Imam.’

Na kumfuata Imam hua ni Wajib kwa Maamuma, hata kama Imam kama Imam atakua amesahau na kufanya kosa kuhusiana na Hatua husika, Yaani kwa mfano kama Imam atakua amejisahau katika Rakaa ya pili baada ya Kusujudu kua akae Attahiyat lakini badala yake Akasimama moja kwa moja kwa kughafilika au kusahau, basi Maamuma hua hatakiwi kukaa kitako, bali anatakiwa na yeye asimame kwa ajili ya kumfuata Imam.’

Na hii ni kama tulivyoona katika Mfano wa Hadith Ya Dhul Yadayn ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisalisha Sala ya Al Asr na kutoa Salam badala ya Rakaa 2 ambayo inasema: '**Abd Allah Ibn Yusuf kua amesema Malik Ibn Anas kua amesema Ayoub Al Sakhtiyani kua:**

عن أبي هُرَيرَة رَضِيَ اللهُ عَنْه، قال صلَّى بنا رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم إحْدَى صلاتَيِ العشيِّ – سمَّاها أبو هريرة، ولكن نسيتُ أنا– قال: فصلَّى بنا ركعتينِ، ثم سلَّمَ، فقام إلى :قال ابن سِيرين خشبةٍ معروضةٍ في المسجِدِ، فاتَّكأَ عليها كأنَّه غَضبانُ، ووضَعَ يَدَه اليُمنى على اليُسرى، وشبَّكَ بين أصابعِه، ووَضَع خَدَّه الأيمنَ على ظَهرِ كفِّه اليُسرى، وخرَجتِ السَّرَعانُ من أبوابِ المسجدِ، فقالوا: وعُمرُ، فهابَا أن يُكلِّماه، وفي القومِ رجلٌ في يديه طولٌ، يُقال قَصُرتِ الصَّلاةُ؟ وفي القومِ أبو بكرٍ له: ذو اليَدينِ، قال: يا رسولَ الله، أَنسيتَ أمْ قَصُرَتِ الصَّلاةُ؟ قال: لم أَنسَ ولم تَقصُر! فقال: أكَمَا يقولُ ذو اليدين؟ فقالوا: نعَمْ، فتقدَّم فصلَّى ما تَرَك، ثم سَلَّم، ثم كَبَّر وسجَدَ مِثلَ سُجودِه أو أطولَ، ثم رفَعَ رأسَه وكبَّر، ثم كبَّر وسَجَد مِثلَ سجودِه أو أطولَ، ثم رفَع رأسَه وكبَّر. فربَّما سألوه (أي: سألوا ابنَ سيرينشم سلَّم؟ فيقول: نُبِّئتُ أنَّ عِمران بن حُصَينٍ، قال: ثم سَلَّمَ

Amesema Muhammad Ibn Sirin kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha moja kati ya Sala za Jioni (Ambapo Imam Ibn Sirin anasema kua Abu Hurayrah Aliitaja Sala hio ila mimi nimeisahau) na akaihitimisha Sala hio baada ya Kuisalisha kwa Rakaa mbili tu. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akanyanyuka na kusimama kwenye karibu na Kigogo kilichopo mbele ya Msikiti na kuuweka mkono wake juu yake huku akiwa anaonekana kama kwamba amekasirika, akauweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto na kuvipitisha vidole vyake vya kulia baina ya vidole vyake vya kulia.

Ambapo Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* hawakuweza kusema chochote kutokana na kumuogopa na kumuheshimu *Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam*. Na wale Masahaba waliokua na Haraka wakaharakisha kutoka Nje, Huku wakiulizana kwa kusema: 'Vipi Leo Sala imefupishwa au?'

Hivyo Kuna Mtu aitwae Dhu Al Yadayn akamsogelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuuliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah Hivi Leo Sala Imefupishwa au umesahau?'

***Rasul Allah Sallallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La Haikufupishwa na wala Sikusahau.'**

Dhu Al Yadayn *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama haikufupishwa basi kwa hakika itakua Umesahau.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum:*'Hivi Jee Dhu Al Yadayn anasema kweli ama la?'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Naam, anasema Ukweli'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasimama. **Na kusalisha Rakaa mbili zilizobakia ambazo alizisahau, na kisha akatoa Salam na akasema Allahu Akbar na kusjudu Sijdat ya Sahau ilizochukua mda wa kama Sijda za Kawaida au zaidi kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar na kisha Akasema Allahu Akbar na Kusujud tena Sijda ya pili na kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akba**r.'

Ambapo Imam Muhammad Ibn Sirin alipoulizwa kuhusiana na kua 'Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam kumalizia ama la?'

Basi Imam Muhammad Ibn Sirin akasema kua: 'Mimi nimeambiwa na Imran Ibn Husayn *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam'*(Bukhari na Muslim)*

Hivyo Ikabidi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amalizie pamoja na Masahaba *zake Radhi Allahu Anhum* Rakaa 2 zilizobakiana ndio maana Wanazuoni wakasema kua Kama Imam atakua amekaa Jalasat Al Istiraaha basi na Maamuma anatakiwa akae ili asiwe ni mwenye kumkhalifu Imam wake na hivyo kua ni mwenye kuenda kinyume na Sunnah ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama inavyoelezewa katika Hadith ifuatayo:

Amesema Abd Allah Ibn Yusuf kua amesema Malik kua amesema Ibn Shihab kua amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipanda Farasi na akaanguka na kuumia katika Upande wake wa Kulia, hivyo akasali moja kati ya Miongoni maa Sala huku akiwa amekaa kitako.Hivyo Nasi tukasali Nyuma yake huku tukiwa Tumekaa Kitako.

Na baada ya Kumaliza Kusali basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema:Imam amechaguliwa kwa ajili ya Kufuatwa, hivyo atakapokua anasali huku amesimama basi na nyinyi Simameni, na atakaporukuu basi na nyinyi Rukuuni, na atakaponyanyua Kichwa chake basi nanyo nyanyueni vichwa vyenu. Atakaposema Sami AllahuLiman Hamida basi nanyi semeni Rabbana wa Laka Al Hamdna atakapokua amesali huku akiwa amekaa iitako basi na nyie salini miiaa mmekaa Kitako*(Sahih Bukhari)***

Na anasema Al Humaidy *Radhi Allahu Anhu* kua:**'Haya maneno ya Hadith hii yasemayo kua: Imam Atakaposali huku akiwa amekaa Kitako basi na Nyinyi kaeni '*Yamebatilishwa Kihukumu*'Na hii ni kwa sababu Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam mwenyewe mwishoni mwa Uhai wake alipokua anaumwa, basi alisalisha huku akiwa amekaa Kitako,lakini Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wao wakasali huku wakiwa wamesimama**.'

Hivyo Hadith hii ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ni Sahih,na inabeba Hukumu ya kua Maamuma anatakiwa Amfuate Imam katika kila hali.Isipokua, Katika hii hali iliyotajwa mwisho kwenye Hadith ambayo ni yenye kuzungumzia kukaa, ambapo hata hivyo amrisho hilo lilibatilishwa mwishoni mwa uhai wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, ambae alisasha akiwa amekaa na Maamuma wakasimama.

Ambapo Anasema Imam Ismail Al Bukhari baada ya kuinukuu Hadith hii kua: **'Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* amesema kua hadith hii kua imebatilishwa kwani Mara ya mwisho *Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam* alisali huju akiaa amekaa kitako na Watu wakasali Nyuma yake huku wakiwa wamesimama.'**

Ambapo kwa Upande wa Mujaddid Ad Din Imam Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Asqallani basi yeye anasema kua: **'Hadith hii (ya Al Humayd) inatumiwa kama Ushahidi wa kubatilisha amrisho la**

Maamuma kusali huku akiwa amekaa Kitako katika wakati ambao Imam amekaa Kitako, kwa sababu baadae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaruhusu Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum*Kusali wakiwa wamesimama huku yeye mwenyewe akiwa amekaa kitako, na huo ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii na Abu Hanifa, Abu Yusuf na Al Awzai.'

Ambapo kwa upande wa Al Walid Ibn Muslim yeye amenukuu kutoka kwa '**Malik na Ahmad Ibn Hanbal amekataa batilisho hilo la amrisho hilo na hivyo amezichanganya Hadith mbili hizi na kuzitumia katika Mazingira mawili tofauti**

Kwani amesema pia Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu kua : Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

انما جعلالامامليوتمبهفلاتختلفواعليهفاذكبرفكبرواولاتكبرواحتيكبرواذركعفاركعواولاتركعواحتيركعواذافلسمعا

للهلمنحمدفقولواربناولكالحمدواذاسجدفاسجدواولاتسجدواحتيسجدواذاصلىجالسافصلواجلوساجمع

ون

***Tafsir:* Imam Amechaguliwa kwa ajili ya kufuatwa, hivyo msipingane nae, atakapofanya Takbir basi nanyi Fanyeni Takbir,Na Msifanyr Takbir hadi Atakapofanya yeye Takbir, Atakaporukuu basi nanyi Rukuuni, wala Msirukuu Hadi Atakaporukuu yeye, Atakaposema Sami Allahu Liman Hamida, basi Nyinyi semeni Rabbana wa Laka Al Hamd, Atakapo Sujudu basi nanyi Sujuduni wala Msisujudu Hadi Atakaposjudu yeye na Akisali akiwa amekaa basi nanyi kaeni** *(Bukhari Na Muslim)*

Ambapo hapa kwanza tunakumbushana tena kua Sehemu ya Hadithi Hii kuhusiana na Imam Kusali akiwa amekaa nanyi Kaeni, imebatilishwa hivyo Hukmu yake haifanyi kazi. Kisha tunapoiangalia Hadith ambayo inafanana na ile tuliyoiangalia hapo kabla basi tunaona kua Hadith zote mbili hizi katika Kuevielezea vitendo hivi vya Ndani ya Sala vinavyofanywa na Imam vinavyotakiwa vifuatwe na Maamuma, basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametumia Herufi 'Fa' Katika kuelezea kila Kitendo.

Yaani Aliposema Faidha Kabbar Fakbiru - Atakaposema Takbir Imam Basi Nanyi Semeni TakbirWaidha Rakauu Farkau, Atakaporukuu basi Rukuuni na Waidha Sajad Fasjadu Atakaposujudu Basi Sujudini

Kwani Herufi Fa hii iliyoanzia katika kuainisha kitendo hua Inaashiria kua Kitendo husika kinatakiwa kifuatwe na kutekelewa kwa haraka bila ya kupoteza mda.

Kwa maana hio basi Amrisho la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Kumfuata Imam katika Sala, ambapo ingawa Hukmu hii hapa sisi mimi nawe tunaitumoa kwa kufahamishana kuhusiana na Ibada ya Sala baina ya Imam na Maamuma, lakini pia Hukmu hii hua haitumiki katika Sala tu, bali hua inatumika katika Sehemu yeyote na katika Jambo lolote linalohusiana na Imani ya Dini ya Kiislam.

Pale inapokua katika Kundi la Waislam au Jamii husika ya Kiislam Ina Kiongozi Mcha Mungu na Muadilifu katika Utekelezaji wa Majukumu yake, hivyo Inapokua Kuna Kiomgozi kama huyu katika Jamii husika basi Maamrisho yake hua yanatakiwa Kufuatwa na Kutekelezwa kwa Walio chini yake, kwani yeye hua tayari ni Imam wa Jamii Husika.

Hivyo Kumkhalifu Au kupingana nae hua ni kuenda kinyume na Hadith hii ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na pia kuenda kinyume na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kulingana na Aya ya 59 ya Surat An Nisaa ambayo inasema:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِى ٱلأَمْرِ مِنْكُمْ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِى شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلآخِرِ ذٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلاً﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo ateeAAoo Allaha waateeAAoo alrrasoola waolee al-amri minkum fa-in tanazaAAtum fee shay-in faruddoohu ila Allahi waalrrasooli in kuntum tu/minoona biAllahi waalyawmi al-akhiri dhalika khayrun waahsanu ta/weelan*(Surat An Nisaa 4:59)*

*Tafsir:**Enyi Mlioamini, Mtiini Allah, Mtiini Mtume(Salallahu Alayhi wa Salam na Watiini wenye Amri Juu yenu miongoni mwenu. Na kama mkitofautiana chocohe kile miongoni mwenu basi rudini kwa Allah Subhanah wa Ta'ala na Mtume wake Salallahuu Alayhi wa Salam, Kma kweli nyinyi ni wenye kuamini juu ya siku ya Mwisho basi kufanya hivyo hua ni bora zaidi kwa ajili ya makazi mema ya mwisho.***

Na hivyo bila ya Shaka Imam hua ni mwenye Amri juu ya Waumini na ndio maana akatakiwa Afuatwe.

Hivyo tunaporudi katika Ibada ya Sala basi amrisho la Hadith linatuonesha kua Hua ni Bora zaid kwa Maamuma kutochelewa katika Kufuata Hatua za Sala nyuma ya Imam wake, kwani anatakiwa aharakishe na wala asipingane nae.

Katika kufahamishana Kuhusiana na Hatua za Ibada ya Sala kulingana na Vithibitisho vya Hadith na Mitizamo ya Wanazuoni basi tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha na kusisitiza Umuhimu wa Kumfuata Imam katika Ibada ya Sala bila ya Kupingana nae.Hata kama akiwa amekosea, na bila ya shaka kimaumbile kila Kiumbe hua ni mwenye kua na Kasoro kwani mkamilifu ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu pekee.

Hivyo basi kwa kua na Imam ni kiumbe basi hua ni mwenye kukosea pia. Na Kiislam ni kua Mtu anapokosea hua ni mwenye kuhitajika kukoselewa, hususan inapokua jambo husika ni lenye kuhusiana na Ibada ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametufundisha namna ya kukosoana ndani ya Ibada ya Sala, kutokana na moja kati ya Matukio yaliyotokea katika Uhai wake, pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam alipokua Maamuma katika Ibada ya Sala ambayo Imam wake alikua ni Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kama inavyoelezewa na Hadith ifuatayo:

عن سهل بن سعد الساعدي رضي الله عنهما أن رسول الله صلى الله عليه وسلم بَلَغَهُ أن بني عمرو بن عوف كان بينهم شَرٌّ، فخرج رسول الله صلى الله عليه وسلم يصلح بينهم في أناس معه، فحُبِس رسول الله صلى الله عليه وسلم وحَانتِ الصلاة، فجاء بلال إلى أبي بكر رضي الله عنهما

يا أبا بكر، إن رسول الله صلى الله عليه وسلم قد حُبِس وحَانت الصلاة فهل لك أن تَؤُمَّ :فقال ، نعم، إن شِئت، فأقام بلال الصلاة، وتقدم أبو بكر فكبَّر وكبَّر الناس، وجاء رسول الله :قال الناس؟ صلى الله عليه وسلم يمشي في الصفوف حتى قام في الصفِّ، فأخذ الناس في التَّصْفيقِ، وكان أبو بكر رضي الله عنه لا يَلْتَفِتُ في الصلاة، فلما أكثر الناس في التَّصْفيقِ الْتَفَتَ، فإذا رسول الله صلى الله عليه وسلم فأشار إليه رسول الله صلى الله عليه وسلم فرفع أبو بكر رضي الله عنه يَدَهُ فحمد الله، ورجع القَهْقَرَى وراءه حتى قام في الصف، فتقدم رسول الله صلى الله عليه وسلم فصلى للناس، أيها الناس، ما لكم حين نَابكم شيء في الصلاة أخذتم في » :فقال فلما فرغ أقبل على الناس، فإنه لا يسمعه أحد سبحان الله، :من نَابه شيء في صلاته فليَقُل .إنما التصفيق للنساء !التصفيق؟ ما مَنَعَك أن تصلي بالناس حين أشَرْتُ :يا أبا بكر سبحان الله، إلا التَفَتَ، :حين يقول ما كان ينبغي لابن أبي قُحافة أن يصلي بالناس بين يدي رسول الله صلى :فقال أبو بكر ،«إليك؟ الله عليه وسلم.

Amesema Sahl Ibn Saad Al Saidi *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alienda kukutana na Watu wa Kabila la Banu Amr kwa ajili ya Kuwapatanisha kutokana na Ugomvi uliotokea Miongoni mwao

Na wakati huo ulikua ni Wakati wa Sala, hivyo Muadhini akamfuata Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu na* Kumwambia: 'Jee Utatusalisha kama nikikimu Sala?'

Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Naam.'

Hivyo Sala ikakimiwa na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akaanza kusalisha Sala, na Watu wakawa wameshaingia Katika Sala wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliporudi, na kujiunga katika Safu.

Hivyo Watu wakaanza kupiga Makofi *(Kumshitua Abu Bakr Radhi Allahu Anhu kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam yupo Mskitini na amrkua Maamuma katika Sala hio Yaani walikua Wanaona kua Abh Bakr anatakiwa ampishe Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam asalishe).*Lakini Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alikua amezama kwenye Sala, hivyo makofi hayo hakuyajali

Masahaba Wakapiga Makofi kwa sauti na kwa wingi zaidi, na hapo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akaeguka na kumuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akataka Kuondoka katika sehemu ya Uimam ili ampishe *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* asalishe yeye, lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuashiria kwa Mkono kua abakie hapo hapo na aendelee kusalisha.

Lakini hata hivyo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akanyanyua Mikono yake juu na Kumshukuru *Allah Subhanah wa Ta'ala*kwa kupewa nafasi hio, na kisha Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu*Akajivuta kutoka katika Sehemu ya Uimam hadi akafikia pembeni kati kati ya Safu, na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasogea mbele na Kuendelea Kusalisha Sala hio.

Mara baada ya Sala hio kumalizika basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu:* 'Jee ni kitu gani kilichokufanya wewe usibakie katika Uimam kama nilivyokuashiria?'

Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akasema: Haistahiki kwa Mtoto wa Quhafa kusalisha na Kua Imam mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawageukia watu na kuwaambia: 'Na Nyinyi kwanini nikakuoneni mkipiga Makofi kwa nguvu sana?'**

Hivyo Sikilizeni kitakapotokea Kitu chochote kile katika Sala, basi semeni Subhanah Allah! Kwani kusema Subhanah Allah kutamfanya Mhusika ajali kwa Umakini, kwani kupiga Makofi Hua ni kwa Ajili ya Wanawake*(Sahih Muslim)*

Kwani hio ni katika Hatua za vitendo vya Sala hivyo kama Imam atakosea Katika Kisomo basi Maamuma hua anatakiwa Amrekebishe kwa kuisoma Aya husika Kiusahih kwa Sauti

Kama Imam ikiwa bado hakufaham basi itabidi afahamishwe baada ya kumalizika Sala, na Kama ikiwa Maneno Aliyoyatamka yameenda kinyume na maana ya Aya stahiki basi Sala hio itabidi Irudiwe Upya Na pia hua inaruhusika kumgutua au Kumjuulisha Mtu kua Unasali kwa kusema kwa Sauti *'Allahu Akbar!' au 'Sami Allahu Liman Hamida!'* Lakini kwa nia ya kua kufanya hivyo ni kwa ajili ya Dhikr

Kwani anasema alivyofafanua Imam Al Khatib Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shirbini kua:'**Ufafanuzi wa Hadith unajumuisha pia katika kusema Allahu Akbar Au Sami Allahu Liman Hamida kwa Sauti, kama ikiwa Mtu anaesali atasema kwa Ajili ya Dhikr Allah na kumfamisha Mtu kua Anasali na Sala haitobatilika, lakini Mtu akisema tu kwa Sauti kwa nia ya Kuonesha kua Anasali, basi Sala hio Itabatilika.'**

NAMNA YA KUNYANYUKA BAADA YA JAALASAT AL ISTIRAAHA

❖❖❖

Kwani tulizungumzia kuhusiana na Namna ya Kuingia kwenye Sujud baada ya kutoka kwenye Kisimamo, na tumeona kua Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kua wao wanasema kua: '**Katika Hatua za Kusujudu basi kwanza Mtu hua anatakiwa aweke Magoti chini kabla ya kuweka mikono yake.'**Ambapo Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Abu Hanifa na Madhhab yake.

Na pia kuna Mtizamo mwengine wa pili usemao kua:**'Katika Hatua za Kusujudu basi kwanza Mtu hua anatakiwa atangulize Mikono yake kisha ndio Magoti yake'**. Ambapo huu ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Al Awzai na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Hivyo umewadia wakati Wa kuangalia kuhusiana na hali inavyotakiwa iwe kwa Mtu anaesali pale anapotoka kwenye Sujud na Kukaa Jalasat Al Istraaha na Kisha anapotaka Kunyanyuka kuingia kwenye

Kisimamo, jee anatakiwa afanyeje?Kwani hapa pia kuna Suali ambalo linasema Hivi Jee Mtu anaponyanyuka kutoka katika Sujud na kutaka kusimama anatakiwa kwanza Anyanyuke kwa kuielemea Mikono yake kujielemeza Ardhini au anyanyuke kwa kuelemea Kutumia Magoti yake moja kwa moja na kuja juu bila ya kutumia Mikono yake?

Ambapo katika hatua hii ya Sala pia Wanazuoni wametofautiana Juu kimtizamo juu ya Jambo hili Kwani kuna Mtizamo wa kwanza ambao ni wenye kusema:

‘Mtu anapotoka kwenye Kwenye Sujud au Jalasat Al Istiraaha au kwenye Attahiyat ya kwanza na kutaka kusimama basi anatakiwa asimame kwa kuegemea Magoti yake na kuja juu bila kujishikiza kwa mikono Ardhini.’

Na wenye Wanazuoni Mtizamo huu basi wao wanasimamia kwenye Hadith ya Wail Ibn Hujayr *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: **'Mimi nimemuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pale alipokua Akiingia kwenye Sujud kua ni mwenye Kutanguliza Magoti yake kwanza kabla ya Mikono, na alipokua Akinyanyuka kutoka kwenye Sujud alikua akinyanyuka kwa kuelemea Magoti yake na Mapaja yake'** *(Sunan Abu Daud, Sunan Imam At Tirmidhii)*

Na kisha kuna Mtizamo wa Pili ambao unasema kua: ‘**Mtu anapotoka kwenye Kwenye Sujud au Jalasat Al Istiraaha au kwenye Attahiyat ya kwanza na kutaka kusimama basi anatakiwa asimame huku akijishikiza kwa mikono Ardhini.’**

Ambapo wenye Mtizamo huu basi wao wanasimamia kwenye Hadith ya Malik Ibn Huwayrith *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: **'Pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua Akinyanyua Kichwa chakr kutoka Ardhini kutoka katika Sijda ya Pili, alikua akikaa kitako Ardhini na kisha Hunyanyuka kwa kuiegemea ardhi na kuja Juu, na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliniambia kua Sali kama Ulivyoniona mimi nikisali'***(Imam Bukhari)*

Na amesema pia Abd Rahman Ibn Yazid Ibn Jabir kua:**‘Nimemuangalia Mimi Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* namna alivyokua Akinyanyuka Kutoka katika Sijda zake baada ya Rakaa ya Kwanza ambapo hua hakai Kitako bali hunyanyuka na kuja juu Moja kwa Moja.’**

Ambapo kunyanyuka moja kwa moja kwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kulikoelezewa hapa hua kunamaanisha kua, alikua alikua hatumii Mikono yake kwa kushika kwenye Ardhi katika kunyanyuka kwake,Na hivyo hii humaanisha kua Mtu hua anatakiwa Kunyanyuka kwa kuinyanyua Mikono kwanza kutoka Ardhini kabla ya Magoti katika Kunyanyuka kwake.

Na hii ndio njia ya Kimaumbile ambayo kila Ibn Adam hua ni mwenye kufanya Pale anaponyanyuka kutoka katika kukaa kitako Ardhini.Ambapo huu ndio Mtizamo wa Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Abd Rahman Ibn Abi Layla, Imam An Nakhai, Imam Abu Said Al Khdhri, Wafuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Naamesema Imam Muhammad Ibn Muslim kua: **‘Mimi nimemuona Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* pale alipokua akinyanyuka baada ya Kusujudu alikua akinyanyua Magoti yake kwanza kabla ya Kunyanyua Mikono yake kutoka Ardhini’** *(Al Tahdhib)*

Hivyo ingawa ile njia ya kwanza ya **‘Mtu anapotoka kwenye Kwenye Sujud au Jalasat Al Istiraaha au kwenye Attahiyat ya kwanza na kutaka kusimama basi anatakiwa asimame kwa kuegemea Magoti yake na kuja juu bila kujishikiza kwa mikono Ardhini.’** ndio ya Kimaumbile lakini njia hii ya pili ya : ‘**Mtu anapotoka kwenye Kwenye Sujud au Jalasat Al Istiraaha au kwenye Attahiyat ya**

kwanza na kutaka kusimama basi anatakiwa asimame huku akijishikiza kwa mikono Ardhini.' ndio njia yenye Kuonesha Unyenyekevu zaidi kwa Mja mbele ya Mola wake na pia humfanya Mtu anaenyanyuka asipoteze usawa wake kutakakompelekea kuyumba katika kunyanyuka kwake.

Na Utumiaji wa njia hii ya Kunyanyuka ndio Mtizamo wa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*, Umar Ibn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhu*, Imam Malik Ibn Anas, Imam Idris Ibn Muhammad Al Shafii, Imam Is-haq Ibn Rahawayh na kauli moja ya Imam Ahamd Ibn Hanbal.Kama alivyosema Mwenyewe Imam Muhammad Idris Al Shafii katika *Al Umm.*

Kwani anasema Imam Is-haq Ibn Rahawayh kua: **'*Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* ametuwekea mfano wa namna ya kunyanyuka kutoka katika Sujud kuingia kwenye kisimamo kwa kujielemeza ardhini wa kutumia mikono iwe mtu huyo awe Mzee au Kijana'***(Marwazi Masail, Al Irwaa)***

Na Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii amesema kua: **'Imam Ahmad Ibn Hanbal alikua akinyanyuka kutoka kwenye Sijda na kusimama alikua akiegemea mikono yake.'**

Ambapo amesema Imaam Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Hanbal katika kumnukuu baba yake kua:**'Kuhusiana na umuhimu wa mjumuiko wa kukaa na kuelemea Ardhi kwa mikono, basi tunaweza kusema kua; kama tukisema kua Mtu amekaa katika Jalasat Al Isiraaha na kuielemea Ardhi hususan mtu husika akiwa ni Mtu Mzee basi mwenye kufanya hivyo hua ni kutokana na Udhaifu wake kiafya au kiumri, na kama ikiwa atanyanyuka kutoka katika kikao chake bila ya kukaa, basi hua ni mwenye kunyanyuka moja kwa moja huku akiwa ni mwenye kuelemea magoti yake.'**

Na anasema Imam Firazbadi Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii katika kitabu chake cha Al Muhadhdhab fi Fiqh Al Imam Al Shafii kua: '**Na utapenda kutegemea Mikono yako kabla ya Kunyanyua Mikono yako pale utakaponyanyuka Kutoka katika Sujud ya Pili, au kutoka katika Jalasata Al Istiraaha, na hii ni kulingana na Wanazuoni wetu wote wa Madhhab yetu**. **Na Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* na Umar Ibn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhu*,na Al Shafii, Na Ahmad na Is-haq,na hii ni kwa sababu ya kutokana na Hadith ya Malik Ibn Huwairih *Radhi Allahu Anhu*pale alipoielezea Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua:Pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam anaponyanyua kichwa chake kutoka kwenye Sujud ya mwisho ya katika Rakaa ya kwanza basi hukaa sawia, kisha hunyanyuka kwa kutegemea Ardhi kwa Mikono yake.'**

Ambapo hivyo ndivyo pia ilivyoelezwa katika kuainisha Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii juu ya hatua hii ya Kunyanyuka kutoka katika Sijda ya Pili ya Rakaa ya kwanza katika vitabu vya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kuanzia katika Al Umm, Al Muhadhdhab,Al Muntaqa cha Imam Al Baji, Al Mughni, Al Sharh Al Kabir, Al Muharara fi Al Fiqh, Al Jawhar Al Naqi n.k.

KUKANDA UNGA BAADA YA JAALASAT AL ISTIRAAHA

❖❖❖

Kwani anasema Malaa Ibn Asad kua: **'Amesema Wahb kua amesema Ayub kua amesema Abu Qilabah kua: Malik Ibn Huwayrith *Radhi Allahu Anhu* alikuja kwetu na kutuongoza kwenye Sala ndani ya Msikiti wetu huu, na akasema: Nakuongozeni katika Sala, lakini mimi sitaki Kusali ila nataka kukuonesheni namna alivyokua Akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.***

Ayoub akasema: Mimi nikamwambia Abu Qilabah, Hivi Jee ilikuaje Sala yake hio?

Abu Qilabah akajibu: Ilikua kama Sala ya Shaykh wetu - Imam Amr Ibn Salamah.'

Ayoub anaendelea kusema kua: Shaykh wetu alikua akimaliza Takbir, na kisha anaponyanyua kichwa kutoka katika Sijda ya Pili alikua akikaa Kitako,Kisha Huielemea Ardhi(Kwa Mikono yake) na Kisha Hunyanyuka.'*(Imam Al Bukhari)*

Na kama tulivyoona kua Hadith hii ambayo ndio inayotumiwa na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Imam Malik, Imam Is-haq Ibn Rahawayh n.k katika uthibitisho wa kua Mtu unaponyanyuka Kutoka katika Sujud Kuja Juu kua unatakiwa Uiegemee Ardhi kwa Viganja na Matumbo ya Vidole vyako kisha unanyanyua Magoti na Kusimama.

Hadithi hii pia Inatuonesha namna alivyokua Akisali Imam Amr Ibn Salamah ambavyo ndivyo alivyokua akisali Malik Ibn Huwayrith *Radhi Allahu Anhu* kua ndio kama alivyokua Akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huku ikiweka wazi namna alivyokua Akinyanyuka *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutoka katika Kikao cha Jalasat Al Istiraaha.

Na vile vile kwa upande mwengine basi Hadith hii Imenukuliwa na Imam An Nasai, kutoka kwa Al Thaqafi kupitia kwa Khalif Al Khadha kupitia kwa Abu Qilabah ambae amesema kua**: 'Wakati Malik Ibn Huwayrith alipokua akinyanyua Kichwa chake kutoka kwenye Sujud ya Pili basi hua ni mwenye kukaa Kitako kidogo na kisha Hunyanyuka Huku akitegemea Ardhi.'**

Wakati amesema Imam Abu Qasim Sulayman Ibn Ahmad Ibn Ayub Ibn Mutayyir Ibn Lakhmi Ash Shami At Tabaranikatika Al Awsat kua:**'Amesema Al Haytham kua amesema Atiyya Ibn Qays Ibn Thalabah kua amesema Al Azraq Ibn Qays Mimi nilimuona Abd Allah Ibn Umar Radhi *Allahu Anhu* akinyanyuka kutoka katika Sujud huku Akiwa Kama anakanda Unga (yaani Mikono yake kaikunja Ngumi), hivyo nikamuuliza: Ndio Umefanya Nini?'**

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema: '**Mimi Nimemuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akikanda* Unga katika Sala.Ambapo Kukanda Unga hua ni Kunyanyuka huku ukitegemea Viganja vya Mikono vikiwa Umevikunja katika Hali ya Ngumi.'***(Al Awsat)*

Naam..kuna Watu ambao Wanaponyanyuka kutoka katika Sujud hua ni wenye Kufunga Ngumi Viganja vyao na kisha kujinyanyua kama Mtu anaepiga Push Up mikono Imefunga Ngumiwakati Wanasema Wanazuoni kuhusiana na aina hii ya Unyanyukaji kua, Unyanyukaji Sio katika Sala, kwa sababu hii hadith iliyotumiwa na Imam At Tabrani ni Hadith Dhaif kwani huyu Al Haytham Ibn Imran ni Mtu asiejulikana na Maneno yanayosema Kukanda Unga ameyaweka yeye.

Kwani anasema Imam Abu Bakr Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abi Shaybah kua: '**Amesema Waqi Ibn Jarrah kua amesema Hammad Ibn Salamah kua amesema Al Azraq Ibn Qais kua:Mimi nimemuona Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua akisimama katika Sala yake kutoka kwenye Sujud huku akiwa ameegemea Mikono yake'***(Musannaf Ibn Abi Shaybah)*

Hivyo amesema Imam Abu Amr Uthman Ibn Abd Rahman Salah Din Al Kurdi Ibn Salah Al Shahrazuri Al Shafii kua: '**Hadith hii Haijulikani na Sio Sahih, na Haikubaliki kutumiwa kama Uthibitisho, mbali ya kua wengi sana miongoni mwa watu wa Uajemi wanaitumia, kwani huu ni uthibitisho wa kitendo kisichokua Halali na kisichojulikana ndani ya Sala'***(Sharh Mushkil Al Wasit)*

Na ingawa Shaykh Albani amesema Hadith hii ni hasan Hadith, lakini Imam Ibn Rajab Al Hanbal amesema pia kua Hadith hii ni Dhaif, Imam Ahmad Ibn Ahmad Ibn Abi Hamid Al Adawi Maliki pia amesema kua ni Hadith Dhaif.

Ambapo kwa upande wa Shaykh Al Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi basi yeye anasema kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akinyanyuka kutoka katika Sujud alikua akiegemea Mikono yake kwa kuweka viganja vyake na matumbo ya vidole vyake Ardhini, hilo halina kupingana juu yake.Ama kuhusiana na Hadith zilizotajwa na kusema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam alikua akinyanyuka kutoka kwenye Sujud na kusimama huku akiwa amekunja Ngumi mikono yake basi ni Hadith Dhaif, Hadith sio za Kweli na Hadith zisizokua na Msingi'***(Sharh Al Muhadhdhab)***

Na katika kusisitiza zaidi basi Imam An Nawawi ameyarudia tena maneno hayo katika Al Tanqih, na kisha Imam An Nawawi akasema katika Sharh Al Muhadhdhab kwa kumnukuu Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii alipoelezea kuhusiana na neno Al Aaajani (Kukunja Ngumi) ambalo ndio Lililotumika katika Hadith hio kua:

'Kama alivyosema Imam Al Ghazal katika kusomesha kwake kua, Kama ikiwa neno hili lina Herufi Zey yaani Aajazi au herufi Nun yaani Aajani. Maana sahih ya Aajani hua ni Mtu anaefunga Ngumi na kisha Kusimama huku akiziegemea Ngumi hizo. Na hivyo kama Hadith hii itakua Sahih basi itakua inamaanisha Mtu anaesimamia Mikono yake kama vile afanyavyo Mtu mwenye Udhaifu wa mwili katika Kuitegemea Mikono yake katika Kunyanyuka kwake, ambalo hili hua ni jambo linalofanywa na Mzee, na hivyo hua haimaanishi Kukanda Unga.'

Imam Al Ghazali anaendelea kusema kua: **'Kama tukisema kua Neno hili lina Herufi Zey, basi hapa itakua inamaanisha Mtu Mzee sana ambae anaposimama hua ni mwenye Kutumia Nguvu nyingi sana, kwani hua ni mwenye kutegemea Mikono yake katika Kusimama kwake kutokana na Uzee wake.'**

Ambapo anasema Imam Ibn Salah kuhusiana na Kauli hii ya Hujjat Ul Islami Imam Al Ghazal kua:**'Kama Sifa za kuuelezea Uzee wa Mtu hua inachukuliwa Mithili ya Mkanda Unga basi hii hua ni kutokana na Kutegemea Sana mikono yake,na wala si kutokana na Kufunga Ngumi Mikono yake.**
Kwani Imam Al Ghazali amesema kua kama ikiwa neno limetumia Herufi Zey, basi hua inamaanisha kua mhusika ni Mtu mzima ambae anaegemea Mikono yake katika Kunyanyuka kwake kutoka Ardhini na hivyo kama Mtu atakua anafanya hivyo kutokana na Uzee wake basi hua Inakubalika kisharia *kwa sababu ya Uzee wake.'*

Naam..anasema Imam Al Bayhaqi kua: **'Tumenukuu kutoka kwa Abd Allah Ibn Umar Radhi Allahu Anhu kua, alikua akielemea Mikono yake katika Wakati wa Kusimama kutoka katika Jalasat Al Istiraaha, na hivyo Ndivyo pia alivyokua akifanya Al Hasan na wengi miongoni mwa Tabiina ndivyo walivyokua wakifanya'***(Sunan Al Bayhaqi)*

Na amesema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: **'Hua ni Sunna kuelemea Mikono yako katika Kunyanyuka kutoka katika Jalasat Al Istiraaha. '***(Al Umm)*

Ama hapa katika Kusimama kutoka katika Jalasat Al Istiraaha pia kuna Masuali ambalo watu wanaweza kujiuliza ambayo kama:**Kama Mtu akikaa kwenye Jalasat Al Istiraaha Jee Ni Wakati gani Mtu huyo hua anatakiwa Kusema Takbir?**

Kwani ndani yake tukio hili hua kuna Masuali ya aina Tatu zifuatazo:

1-Jee Mtu anatakiwa aseme Allahu Akbar katika Wakati anaotoka kwenye Sijda na kuingia Kwenye Jalasata Al Istiraaha.
Au;

2-Jee Mtu anatakiwa Aseme Allahu Akbar anapoanza kukaa na Kuimalizia wakati anapomaliza Kukaa Jalasat Al Istiraaha.
Au;

3-Jee Mtu anatakiwa Kusema Allahu Akbar katika Wakati ambao ananyanyuka kutoka Katika Jalasat al Istiaaha na Kusimama.

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kuna Mitizamo mitatu tofauti kama ilivyoelezwa na Imam Al Baghawi, Imam Al Mutawwali na Imam Al Shirazi muandishi wa Al Bayyan fi Madhhab Imam Al Shafii Sharh Kitab Al Muhadhdhab.**'

Ambapo Mtizamo Sahih katika Yote kulingana na Wengi miongoni mwa Wanazuoni na Muandishi wa Al Tanbih *(Imam Abu Is-haq Al Shirazi - Al Tanbih Fi Al Fiqh Al Shafii)*Ni kua Mtu anatakiwa anaanza kusema Takbir wakati anapojunyanyua Kutoka kwenye Sijda na Kuivuta hadi katika Kusimama kwake huu akiwa ni mwenye Kukifupisha kikao cha Jalasata Al Istiraaha. **Na hii ni kutokana na Uthibitisho wa waliyoyasema Imam Al Shirazi na Wanazuoni wengineo, kua hakuna hata sehemu moja ya Sala ambayo hua tupu bila ya kua na Dhikr ndani yake.**

Mtizamo wa pili ni kua Mtu anatakiwa anaponyanyuka Kutoka kwenye Sijda asiseme chochote hadi anapofika kwenye Jalasat Al Istiraaha na kisha anaanza Takbir katika Wakati anaponyanyuka kutoka kwenye *Jalasat Al Istiraaha* hadi anaposimama sawia.

Na Mtizamo wa Tatu ni kua Mtu anajinyanyua kutoka kwenye Sijda huku akisema Takbir hadi anapoingia kwenye Jalasat Al Istiraaha. **Na kukaa basi ananyamaza, na kisha ananyanyuka kuja Juu bila ya Takbir, ambapo Mtizamo huu umenukuliwa na Al Qadhi Abu Hamid kutoka kwa Imam Abu Is-haq Al Marwazi na Qadhi Abu Al Tayyib al Tabbari ameupitisha Mtizamo huu**. **Na As-hab al Wujuh wetu wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanasema kua Hakuna kutokukubaliana juu ya kua hapa katika Hatua hii hua haitakiwi kutamka Takbir mara mbili na miongoni mwa Walioweka wazi hilo ni Al Qadhi Husayn na Al Baghawi.***(Al Majmuu)*

Ambapo kwa Upande wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi amesema kua: '**Si jambo zuri Kuirefusha sana Takbir, kwani kufanya hivyo hua kunahitaji uthibitisho kutoka katika Sunna**'*(Al Talkhis)*

Kwani kwa upande wa *Muwwafaq* Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Inapendekezwa kwa Mtu anaesali kutamka Takbir tangu kuanzia kutoka katika Kunyanyua Kichwa kutoka kwenye Sijda hadi kuimaliziaKwenye Kisimamo, na hivyo ndio atakua ni mwenye Kuisimamia nguzo ya Takbir ndani ya SalaNa hivyo ndivyo inavyotakiwa katika Takbir zote Isipokua kwa yule mwenye kukaa Jalasat Al Istiraaha**. **Kwani mwenye kukaa Jalasat Al Istiraaha huanza Takbir yake anaponyanyua kichwa kutoka kwenye Sijda na kuimalizia katika kumalizia jukaa kwake *Jalasat Al Istiraaha*, na hivyo Hunyanyuka kutoka katika *Jalasat Al Istiraaha* na kusimama bila ya Takbir.**'

Na Ingawa Imam Abu Al Khattab amesema kua: Mtu anaetoka kwenye Sujud na kukaa kwenye Jalasat Al Istiraaha. **Hua anatakiwa aseme Allahu Akbar katika Wakati ambao anasimama kutoka kwenye Jalsat Al Istiraaha na kuja Juu Ambapo Mtizamo huu wa Imam Abu Al Khattab sio Mtizamo Sahih, kwani humpelekea Mtu kufanya Takbirat Mbili katika Nguzo Moja ya Sala'** *(Al Mughni ya Imam Ibn Qudamah Al Hanbali)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Mardawi Al Hanbali basi yeye anasema kua:**'Kama ikiwa Mtu atakaa katika Jalasat Al Istiraaha, basi hua ni mwenye kunyanyuka bila ya kusema *Allahu Akbar*, na huo ndio Mtizamo sahih katika Madhhab yetu, kwani kusema kwake *Allahu Akbar* katika kutoka kwenye Sujud kuingia kwenye *Jalasat Al Istiraaha* hua kunatosheleza**. **Na kuna Waliosema kua anatakiwa aseme *Allahu Akbar* katika wakati wa Kusimama, na haya ni maneno ya Imam Abu Al Khattab,hivyo hii ni kauli yake na Wanazuoni wamekaa mtizamo huo.'** *(Al Insaaf)*

Hivyo kama tulivyoona kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Mtizamo unaokubalika zaid na kutegemewa ni kua Mtu unatakiwa kusema *Allahu Akbar* mara tu baada ya kutoka kwenye Sujud na unaingia nayo kwenye Jalasat Al Istiraaha ambapo utakaa kwa mda mdupi tu huku ukiendelea nayo *Allahu Akbar* hadi katika Kusimama kwako na kufunga Mikono kama alivyosema Imam An Nawawi.

Kwani amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisimama kuingia kwenye Sala basi alikua akisema Allahu Akbar, anaporukuu husema Allahu Akbar anapotoka katika Rukuu husema *Sami Allahu liman Hamida,* anaposimama baada ya Rukuu husema *Rabbana wa Laka Al Hamd* Kisha husema Allahu Akbar pale anapoelekea chini kwenye Sujud,husema Allahu Akbar anaponyanyua kichwa kutoka kwenye Sujud, husema Allahu Akbar anaposujudu tena na husema Allahu Akbar anaponyanyua Juu kichwa chake na hufanya hivyo katika rakaa ya Sala nzima.'**(*Bukhari na Muslim)*

Hivyo maneno yasemayo kua Husema *Allahu Akbar* anaponyanyua Kichwa chake na hufanya hivyo katika kila rakaa ya Sala yake yanathibitisha juu ya hili.

Na ingawa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wanasema kua : '**Mtu anatakiwa aseme Allahu Akbar anapotoka kwenye Sijda na kuimalizia pale anapokaa kwenye Jalasat Al Istiraaha.'**

Lakini kwa Upande wa Wanazuoni wa Kisalafi akiwemo Shaykh Al Uthaymin, na Ibn Baz basi wao wameachana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal katika hili na kuamua kufuata Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Kwani wao wanafuata Mtizamo wa Pili wa Madhhab ya Imam Al Shafii usemao kua:**'Mtu hua anatakiwa aseme Allahu Akbar pale anapoingia kwenye *Jalasat Al Istiraaha* na kuja juu nayo katika Kisimamoambapo Al Uthaymin anasema kua:** '**Kama Imam atakaa *Jalasat Al Istiraaha* basi atasema Takbir katika Kunyanyuka kwake kutoka katika *Jalasa Al Istiraaha'***(*Al Liqa Al Maftuh)*

10-TAHIYYAT - TASHAHUD MAANA YAKE NA ASILI YAKE

❖❖❖❖

Neno Attahiyat ni nemo linalotokana na neno la Kiarabu lijulikanalo kama Hayya. Ambapo neno Hayya hua ni lenye kutokana na Mzizi wa Herufi mbili za Kiarabu ambazo ni Ha na Ya.

Hivyo herufi mbili hizi zinapokua pamoja huunda neno Hayya ambalo humaanisha Kua Hai, Kuhuisha, Kukesha, Kunawirisha, Kuzuia Mtu asidhurike, Kumpa heshima Mtu n.kNeno Hayya hua linamaanisha pia Kua na Haya, kuona Haya, kua na Aibu kuona Aibu, na pia humaanisha Kutubu, Na Neno Hayya ndio lililotoa neno Ahyaun ambalo humaanisha Watu wa Peponi. Allah atujaalie nasi kua Pamoja nao..Aamiin.

Neno Hayya ndio pia lililotoa neno Istihyaa ambalo humaanishaKujizuia dhidi ya Kitu, Kujihifadhi dhidi ya Kitu, ambapo neno hili hili Istihyaa linapotumika kwa upande wa Mwanamke basi hua linamaanisha Asiekua na Haya. Na hivyo pia neno Hayya ndio liliyoa neno Hayyatun lenye Kumaanisha Joka kubwa sana lenye Kutambaa kama ilivyokua Fimbo ya Nabii Musa alipokua anaitupa chini.

Hivyo ukweli ni kua Neno Hayya lina maana nyingi sana, na hii ni kutokana Utajiri wa Lugha ya Kiarabu.Kwani neno hilo ndio pia lililotoa neno *Hayyit* lenye kumaanisha Kumuombe Dua mtu ili aishi Maisha Marefu na Mazuri sana hivyo nami namuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atujaalie Sote Maisha Mema na Marefu hapa Duniani ili tupate kuchuma zaidi na kufanikiwa kupata Radhi zake kesho Akhera...Amiin

Na tumalizie maana ya neno Haya kwa kukumbushana kua Hata kile kitabu, kilichompatia Umaarufu wa kupatia Sifa ya *Hujjat ul Islami*(Hoja au Uthibitisho wa Uislam) *Hujjat Ul Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii ambacho sifa yake Kithamani basi ni kua baada ya Qur'an kisha inafuatia Vitabu vya Hadith na Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* basi kinafuatia kitabu chake hicho mwenyewe amekiita Ihya Ulum Ad Diin, Yaani Uhai wa Ilm ya Dini ya Kiislam.

Na Bila ya shaka hakukosea kukipa Jina hilo lenye kutumia neno Ihya lililotokana na neno Hayya.

Na kama tulivyosema kua neno Tahiyyat limetokana na neno Hayya ambalo tumeshalifafanua hapo kabla, na anasema Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami, Sultan Al Mutakkalimin Imam Al Mushaqiqiin Imam Al Ghazali Al Thani ImamAbu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Ibn Al Husayn Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kua: '**Neno Tahiyyat hua linamanisha Kukiheshimisha Kitu, hivyo kila kitendo chenye kupelekea Kitu kua ni chenye kuheshimika hua kinaingia ndani ya Maana ya Neno Atahiyyat'** *(Mafatih Al Ghayb)*

Naam nimetumia maana hii inayotokana na Ufafanuzi wa Imam Fakhr Ad Din Al Razi kwa sababu ya kutaka kufahamiana vizuri zaidi kuhusianana Ibada ya Sala na Kikao na kisomo cha Tahiyyat.Na hivyo tukichukulia maana hii basi moja kwa moja tunaona Darja, Thamani na Umuhimu wa Ibada ya Sala na kila kitendo kinachojumuishwa ndani yake kua ni chenye kuheshimika mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kiasi ya kua Mtu unapokua unasali kwa Ikhlasi basi unakua mbele ya Mola wako na chini yake Mola wako.

Na kila chenye kuheshimiwa basi hua ni chenye kupokelewa kwa Maamkizi ya Heshima.Kama anavyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua Katika Aya iliyotumia mzizi wa neno Hayya katika maneno yake matatu yenye hali tatu tofauti sambamba hapo kwa hapo kua:

﴿وَإِذَا حُيِّيتُم بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّواْ بِأَحْسَنَ مِنْهَآ أَوْ رُدُّوهَآ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ حَسِيبًا﴾

Wa-i<u>dha</u><u>h</u>uyyeetum bita<u>h</u>iyyatin fa<u>h</u>ayyoo bi-a<u>h</u>sana minh<u>a</u> aw ruddooh<u>a</u> inna All<u>a</u>ha k<u>a</u>na AAal<u>a</u> kulli shay-in <u>h</u>aseeb<u>a</u>n*(Surat An Nisaa 4:86)*

*Tafsir:**Mtakapoheshimiwa (salimiwa) kwa Tahiyyat (Maamkizi ya Heshima) basi Salimieni (Rudisheni Heshima ya Maamkizi hayo) kwa Majibu bora zaidi yakeauRudusheni kama Mlivyoamkiwa Kwani kwa Hakika AllahNi Mwenye Kuhesabu Juu ya Kila Kitu**.)*

Na akasema tena katika Kitabu chake hicho kuhusiana na Watu wa Peponi kua:

﴿تَحِيَّتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُۥ سَلَٰمٌ ۚ وَأَعَدَّ لَهُمْ أَجْرًا كَرِيمًا﴾

Tahiyyatuhum yawma yalqawnahu salamun waaAAadda lahum ajran kareeman*(Surat Al Ahzab 33:44)*

*Tafsir: **Maamkizi yao (Kuheshimiwa kwao) Katika Siku hioWatapokewa kwa Salaam'Salaam Alaykum' Na (Allah Subhanah wa Ta'ala) amewahidiaMalipo Ya heshima Kubwa sana.***

Allah atujaalie nasi kua miongoni mwao watu hao....Amiin.

Na akasema tena*Allah Subhanah wa Ta'ala* pia:

﴿وَأُدْخِلَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ جَنَّٰتٍ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ ۖ تَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَٰمٌ﴾

Waodkhila alladheena amanoo waAAamiloo alssalihati jannatin tajree min tahtihaAl anharu khalideena feeha bi-idhni rabbihim tahiyyatuhum feeha salamun*(Surat Ibrahim 14:23)*

*Tafsir: **Na Wataingia Wale WalioaminiNa Wakafanya MemaKatika Mabustani Yenye Kutiririka Chini yake ChemchemWatakaa Ndani yake humoKwa Idhini ya Mola wao na Maamkizi yao (kuheshimisa Kwao)Ndani yake (Peponi humo) Salaam Alaykum.***

Allah atukutanishe sote Kwa Pamoja Peponi..Aamiin

Kwa upande mwengine tunaona kua neno *Tahiyyah* maana yake hua ni *Hayyaka Allah*, yaani Allah Akuweke Hai ambapo haya ni maneno ya maamkizi yaliyokua yakitumika katika wakati wa Ujahiliya katika Ardhi ya Uarabuni kabla ya kuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hivyo kabla ya kuendelea zaidi kuhusiana na hatua ya Kikao na Kisomo cha Attahiyat ndani ya Sala basi tufahamishane kuhusiana na Faida ya Kisomo cha Attahiyat kama utaisoma Nje ya Sala ambapo hii hua ni sehemu ya Ilm ya Mujarrabat, yaani Ilm iliyojaribiwa na Wanazuoni na ikatoa Matokeo Stahiki.

Ambapo tunapoangalia Matumizi ya Kisomo cha Attahiyat katika Upande huo wa Nje ya Sala basi tunaona kua Imejaribiwa na kutoa Majibu kulingana na nia zifuatazo:

1-Ukimsomea Mtoto Mtukutu Kisomo cha Attahiyat mara 41 huku ukimpulizia basi Mtoto huyo ataondokewa na Tabii ya Utukutu na atakua Msikivu kwa Idhini ya *AllahSubhanahwa Ta'ala.*

2-Ukitaka kukiongeza chakula chako Barka yaani kwa mfano Mko watu wengi na Chakula ni kidogo basi wakati unakipika Chakula hicho Kisomo cha Attahiyat 7 na chakula hicho kidogo kitakua na baraka na kuwatosheleza wahusika..*Biidhni Allah.*

3-Kama utadumu nayo kwa kuisoma kila siku baada ya Sala ya Alfajir mara 41 basi Maisha yako yataboreka Kiuchumi *bi Idhini Allah.*

4-Kama una Shamba na unataka Ardhi yake itoe mazao kwa wingi. Basi wakati Unapopanda mbegu zako shambani,basi ukisomea Kila mbegu Attahiyat moja utapata Mavuno mazuri *Biidhni Allah.*

5-Ukizisomea Mali zako na Pesa zako katika Wakati wa Kuzihifadhi basi Mali na pesa hizo zitakua ni zenye Baraka *Biidhni Allah.*

6-Kama Kuna Mwanammke Mja Mzito ambae atakua na Tabia ya Kusoma Attahiyat mara ka mara Kila siku katika Wakati wa Uja uzito wake basi atajaaliwa kujifungua Mtoto Mcha Mungu *Biidhni Allah*.

7-Kama Wanandoa ambao Ndio kwanza wameoana kisha Wakaisoma Attahiyat katika Wakati wanaingia pamoja ndani ya Nyumba yao watakayoishi basi Wataishi maisha ya Mapenzi, Utulivu, huruma na Furaha ndani ya Makazi yao hayo na ndani ya Ndoa yao hio.

Na tunapoendelea katika kuangalia Kikao cha Ndani ya Sala ambacho ndani hua ni Kikao cha Rakaa ya Mwanzo katika kila zenye Rakaa zaidi ya Mbili.

Yaani katika Sala za Fardhi basi hua ni kikao cha kwanza cha Salat Dhuhr, Salal Al Asr, Salat Maghrib na Salat Al Ishaa.Kwa maana hio basi Sala ya Al Fajir ambayo hua ina Rakaa mbili basi hua haina Kikao hiki tutakacho kizunguzmia hapa, kwani Sala ya Al Fajir ina kikao cha Attahiyat ya Mwisho tu, ambayo tutaizungumzia baadae *Inshaa Allah.*

Kwani kikao hiki cha Attahiyat ya Kwanza ya ndani ya Sala hua kinajuiikana pia kama Tashahhud.Hivyo kuna wanaokiita kikao hiki kua ni kikao cha Attahiyat ya kwanza na Kuna wanaokiita kua ni kikao cha Tashshahud ya Kwanza.

Na hivyo Attahiyat ya Pili hua pia inajulikana kama Tashshahud ya Pili.Na zimeitwa hivyo kwa sababu ndani yake mnasomwa kisomo cha Attahiyat ambacho ndani yake mna Uthibitisho wa kushuhudia Imam ya Dini ya Kiislam.

Kwani anasema Imam Al Bukhari kupitia katika Hadith ya Abu Humayd As Saadi *Radhi Allahi Anhu* katika Hadith isemayo kua:

كان رسول الله صلى الله عليه وسلم إذا قام إلى الصلاة يرفع يديه حتى يُحَاذِيَ بهما مَنْكِبَيْهِ ، ثم يُكبِّر حتى يَقِرَّ كل عظم في موضعه معتدلا، ثم يقرأ، ثم يكبِّر فيرفع يديه حتى يُحاذي بهما مَنْكبيه، ثم يركع ويضع رَاحَتَيْهِ على رُكبتيه، ثم يعتدل فلا يَصُبُّ رأسه ولا يُقْنِعُ ، ثم يرفع رأسه، فيقول :سمع الله لمن حمده، ثم يرفع يديه حتى يُحاذي بهما منكبيه معتدلا، ثم يقول :الله أكبر ثم يهوي إلى الأرض فيُجافي

يديه عن جنبيه، ثم يرفع رأسه ويَثْني رجله اليسرى فيقعد عليها، ويفتح أصابع رجليه إذا سجد، ويسجد الله أكبر، ويرفع رأسه ويَثْني رجله اليسرى فيقعد عليها حتى يرجع كل عظم إلى موضعه، ثم :ثم يقول يصنع في الأخرى مثل ذلك، ثم إذا قام من الركعتين كبر ورفع يديه حتى يحاذي بهما منكبيه كما كبر عند افتتاح الصلاة، ثم يصنع ذلك في بقية صلاته حتى إذا كانت السجدة التي فيها التسليم أخر رجله صدقت هكذا كان يصلي صلى الله عليه وسلم :اليسرى وقعد مُتَوَرِّكًا على شقه الأيسر، قالوا

Abu Humayd Al Saadi Akasema: '*Rasul Allahu Alayhi wa Salam* anaposimama Kusali, alikuwa akinyanyua mikono yake sambamba na mabega yake, akitamka Takbir, kisha anasubiri mpaka kila mfupa wa mwili wake utulie sawasawa. Kisha alikuwa akiisoma (Qur'ani), kisha anainua mikono yake sambamba na mabega yake na kusema Takbir, kisha akainama, akiweka viganja vyake juu ya magoti yake, kisha alikuwa akisimama wima akiinamisha kichwa chake bila kukiinua sana kisha anasema: '*Samia Allahu Liman Hamida'* kisha huinua mikono yake hadi usawa wa mabega yake huku akisimama wima Kisha husema Allahu akbar na, huku akiweka mikono yake mbali na ubavu wake, kisha anainua kichwa chake na kunyoosha mguu wake wa kushoto na kuukalia juu yake, na alikuwa akikunjua vidole vyake vya miguu wake wa kulia na hukaa hivyo mpaka kila mfupa urudi mahali pake. Kisha anaposimama baada ya Rakaa mbili, aliinua mikono yake hadi usawa wa mabega yake kama alivyokuwa akifanya mwanzoni mwa Salah. Kisha alikuwa akimalizia sala yake iliyosalia kwa namna hiyo hiyo, na anapofika kwenye sijda inayofuatiwa na Taslim, alisogeza mbele mguu wake wa kushoto na kukaa, huku akiweka makalio yake upande wa kushoto juu ya ardhi." *(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhi)*

Ambapo kwa Upande mwengine basi Imam Ibn Hibban yeye ameinukuu Hadithi hii huku ikiwa ni yenye maneno yasemayo kua: '**Na Hukalia Ugoko wa Mguu wake wa Kushoto katika Hali ya Tawarruk'***(Sunan Al Kubra)*

Na pia kuna Hadith ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akikaa katika Rakaa ya pili basi alikua akikalia Mguu wa Kushoto huku akiusimamisha Unyayo wa Mguu wa Kulia, na alipokua akikaa katika Rakaa ya Mwisho basi huusogeza mbele mguu wake wa kushoto na kuunyanyua mwengine huku akiwa amekalia Makalio yake ardhin**i'*(Fat-Al Barr)*

Kwani kwa upande wa Imam Abu Hatim Muhammad Ibn Hibban Al Busti basi yeye amenukuu pia hadith hii ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* lakini ikiwa na maneno yasemayo:'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akikalia Ugoko wake katika Mkao wa Tawwaruk.'** Ambapo hadith hii pia imenukuliwa na Imam Al Bayhaqi, Imam Ahmad na Imam At Tirmidhii.

Hivyo kutokana na Vithibitisho vya Hadith hii katika hali tofauti basi tunaona Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii pamoja na Imam Al Shafii Mwenyewe wana mtizamo wa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitofautisha baina Attahiyat ya mwanzo na ya Mwisho kwa aina ya mkao anaokaa. Kwani katika Attahiyat ya Mwanzo alikua akikaa Katika Mkao wa Iftirash ambao ni wa kukalia sehemu ya Pembeni ya Unyayo ya Mguu wa Kushoto huku mguu wa Kulia ukiwa umesimamisha Unyayo wake na vidole vyake vikisa vimeelekea Kibla.

Na hivyo katika Attahiyat ya Mwisho basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akikalia mkao wa Tawwarukambao ni wa kuusogeza mbele Unyayo wa Mguu wa Kushoto hadi kuukaribia Mguu wa Kulia, huku unyayo wa Mguu wa Kulia ukiwa umesimama kama kawaida yake na Hivyo Kalio la upande wa Kushoto hua ni lenye kukaa Ardhini.

Yaani utofauti unaokuwepo unakua ni wenye kuweza kumtofautishia Mtu atakaekuja nyuma yake katika Wakati ambao anasali na hivyo kama akimuangalia Nyayo zake zilivyokaa tu basi mtu husika hua anajua kua hii ni Rakaa ya Pili au ni Rakaa ya Mwisho bila ya hata kuuliza.

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Al Hafidh Imam Abu Fadhl Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Hadith ya Abu Humayd *Radhi Allahu Anhu* ni yenye uthibitisho wenye Nguvu kwa upande wa Imam Al Shafii ambae ni mwenye kutofautisha mikao baina Tashahhud ya kwanza na Tashahhud ya Mwisho, kwani inatakiwa ifahamike kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikaa mkao wa Iftirash katika Tashahhud ya kwanza na Tawwaruk katika Tashahud ya mwisho.'** *(Fat-h Al Barr, Al Hafidh Ibn Hajar Al Asqallani)*

Al Hafidh Imam Ibn Hajar Al Asqallani anasema hivyo kwa sababu Wanazuoni wametofautiana juu kikao cha Attahiyat, na hivyo kua ni wenye mtizamo tofauti, kama inavyotuonesha*Mawsuat Al Fiqhiyat Al Quwaytiya* kuhusiana na *Attahiyat* au *Tashahhud*na utofauti wa Mitizamo yake kwa kusema:

1-Madhhab ya Imam Abu Hanifa, basi Wanasema kua kwa upande wa Wanaume, Hua wanatakiwa wakae mkao wa Iftirash katika Vikao vya Tahiyyat ambapo kwa upande wa Mwanamke hua ni Tawarruk.

2-Madhhab ya Imam Malik Ibn Anas basi wao wanasema kua: Kikao cha Attahiyat mtu hua anapendekezwa zaid akae mkao wa Tawarruk kuliko mkao wa Iftirash.

3-Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua katika Kikao cha kwanza cha Tahiyyat basi mtu hua anatakiwa akae katika Mkao wa Iftirash na katika Tahiyyat ya Mwisho anatakiwa akae katika Mkao wa Tawarruk.

4-Madhhab ya Imam Al Shafii basi Mtizamo wao hua hauangalii vipi mtu anakaa katika Vikao vya Tahiyyat kwani Mtu atakavyokaa basi hua hamna tatizoisipokua ni Sunna na Inapendekezwa zaid kua Attahiyat ya mwisho Mtu akae Mkao wa Tawarruk. Kwani anasema Imam An Nawawi kua: Ukweli ni kua Mkao wowote unaofaa atakaokaa mtu katika Kikao cha Tahiyyat basi hua unafaa na kukubalika. Lakini kulingana na Vithibitisho vya Sunnah basi katika Tahiyyat ya mwisho hua ni kukaa Mkao wa Tawarruk na pia kukaa Mkao wa Ifitrash katika Tahiiyat ya Mwisho ya Sala.' *(Al Majmuu)*

Kwani bora tufafanue kidogo hapa aliposema Imam An Nawawi kua ni Sunna kukaa Iftirash na Tawwaruk katika Atahiyat ya Mwisho: '**Kwani hapa imekusudiwa kua Kama Mtu Atakua anasali Sala ya Rakaa mbili basi kikao cha Atahiyyat hua ni kimoja tu cha Mwisho na kitakua katika hali ya Iftirash. Na kama Mtu atakua anasali Sala yenye Tahiyyat ya kwanza na ya mwisho basi Tahiyyat ya kwanza itakua katika Iftirash na ya pili itakua katika Tawarruk.'**

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Hikma iliyomo katika Utofautishwaji wa mikao hii miwili ni kutokana na sababu ya kua Mtu anapokua amekaa katika Mkao wa Iftirash katika Rakaa ya pili basi hua ni rahisi kwake kunyanyuka kuingia kwenye Rakaa ya tatu kuliko akiwa amekaa kwenye mkao wa Tawwaruk ambao hua ni vigumu kunyanyuka. Kwa Hivyo mkao wa Iftirash hua ni kwa ajili ya kurahisisha**

kunyanyuka kuendelea na Sala na mkao wa Tawarruk hua ni kwa ajili ya kikao Atahiyyat ya mwisho ambacho ndani yake mtu hua anaweza kuomba Dua Ndefu kwa kadri awezavyo.'

Na ingawa Imam An Nawawi amesema hivyo pia kuainisha umuhimu wa Madhhab ya Imam Al Shafii wa kusimamia Mtizamo wa Mkao wa Tahiyyat ya kwanza kua ni Iftirash na mkao wa Tahiyyat ya Mwisho kwa ajili ya Sala yenye Rakaa Tatu hadi Nne kua ni Tawwaruk.

Kutokana na kua kufanya hivyo hua ni Sunna ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yenye Hikma kubwa ndani yake.

Lakini hapo hapo pia Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanasema kua: **'Mtu anesali anatakiwa akae katika mkao wa Tawarruk kwa kuzingatia hali ya Mazingira anayosali.'**

Yaani..kama Mtu anasali katika Sala ya Jamaa na kisha Watu wamebanana, kiasi ya kua kutekeleza Sunna ya kukakalia mkao wa Tawwaruk kutuka Tahiyyat au Tashshahud katika Rakaa ya mwisho kutapelekea kuwabana zaidi Maamuma wenzako wanaosali pembeni yako na hivyo kuwasababishia Usumbufu na kuwaondoshea Khushuu Waislam wenzako.

Basi katika hali na mazingira kama haya hua haikubaliki kukaa Mkao wa Tawarruk hata kama ni Sunna, kwa sababu kukaa kwako huko kutasababisha Udhia na Madhara kwa Waislam wenzako na pia utajikosha wewe mwenyewe Malipo sahih ya Sala yako na hivyo katika hali kama hii basi badala ya kukalia mkao wa Tawarruk Hua ni bora kwako kukalia mkao wa Iftirash.

Na tunakumbushana haya kwa sababu kuna watu ambao wanapenda kutekeleza Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, na* ingawa hili ni jambo zuri lakini, tusiwe kama wajinga ambao wanarukia Jambo bila kulijua kwani kufanya hivyo hua ni sawa na Mtu aliekosa Maji kwa mda mrefu akiwa safarini Na kisha alipokutana na Maji Safi yaliyotulia Ardhini basi kutokana na hamu yake na hali aliyokua nayo basi akaamua kujirusha Ndani yake bila kuangalia urefu wa kina cha Maji hayo na matokeo yake mtu huyo kufa maji kutokana na urefu kubwa sana wa kina cha Maji husika.

Hal kadhalika kama ilivyokua kosa la kutopima Urefu wa Kina cha Maji yaliyotulia huweza kumuangamiza Mtu basi pia kutojua Amali husika humpelekea Mtu kujiangamizia Amali zake na hivyo kukosa Malipo ya amali njema yake.

Hivyo kwa wale wenye kupenda kutekeleza Sunnah hii ya mkao wa Tawarruk, basi tunatakiwa tukumbuke kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua katika kila mkao wa Sala akikaa hua ni mwenye kukaa hadi Mifupa yake hunyooka sawasawa kama zilivyosema Hadith ikiwemo katika Mkao huu wa Tawarruk.

Kwa Maana hio basi, unapokaa katika Mkao wa Tawwaruk hakikisha kua Uti wa Mgongo wako unanyooka katika kuusimamisha kwake na ukikaa hivyo basi hutokua ni mwenye kuwakera Maamuma wenzako.

Lakini kama Mtu ukiwa unakaa mkao wa Tawwaruk huku Mgongo wote umeangukia upande wa Maamuma mwenzako wa Kushoto kwako kama vile Tanga la Jahazi lililojaa Upepo wa Kusi, na Uti wako wa mgongo umejipinda kama Upinde ambao umebeba Mshale uliovutwa Sana na unaosubiri Kuachiwa tu! Basi bila ya shaka Mkao huo hautokua mkao wa Tawwaruk, wala hautokua Sunnah, na wala hautoonesha kua Una Khushuu bali itakua Adhaa na utawasababishia usumbufu Maamuma wenzako na Utaandikiwa Dhambi kwa Kuwatoa Khushuu Waislam wenzako.

Na pia utakua Kaslan (Mtu anaesali Kiuvivu kwa Kujiachia bila kujali Sala yake kivitendo wala kimaneno) na hivyo kukukosesha wewe Malipo ya Sala yako.

Na tumemalizana na aina za Mikao ya Tahiyyat/Tashshahud kulingana na mitizamo ya Wanazuoni mbali mbali na tunakaribia kuingia kwenye Maneno yenyewe ya Tahiyyat.Lakini kabla hatujagusa huko basi kwanza kuna kitu muhimu ambacho inabidi tukiweke wazi Na hii ni kwa sababu kitu hicho kinahusiana na baadhi ya Kauli zinazoelezea kuhusiana na Uasili wa Kisomo cha Tahiyyat kwani kuna Wanazuoni walionasibisha Kisomo cha Tahiyyat kua Asili yake inatokana ndani ya Safari ya Miraj ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwani anasema Imam Abu Layth katika *Tanbih Al Ghafilin,* na pia amesema Al Aalamah *Imam Al Muhaddith Al Faqih Badr Al Din Abi Muhammad Mahmud bin Ahmad Al Ayni*kua amesema Imam Farwadi katika Thawabul Ibadat na Imam Al Fihristan Abu Latif Ibn Al Malak katika Kitabu chake cha Mabarik Al Azhar, kua:

روي : أنه ﷺ لما عرج به أثنى على الله تعالى بهذه الكلمات ، فقال الله تعالى : «السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته» ، فقال عليه السلام : «السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين» ، فقال جبريل : «أشهد أن لا إله إلا الله ، وأشهد أن محمدا عبده ورسوله

‘**Katika Usiku wa Miraj wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam alipopandishwa Mbinguni basi alikua akimtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kutumia Sehemu ya kwanza ya maneno ya Tahiyyat, na hivyo*Allah Subhanah wa Ta'ala* nae akajibu kwa kusema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh*. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina*. Na kisha Malaika Jibril akasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu AnNa Muhammadan Rasul Allah.’(**Al Bina’ah fi Sharh Al Hidayah**)***

Na amesema Imam Al Qurtubi katika Tafsir yake ambapo yeye amesema kua:

فأما من قال : إنها كانت ليلة المعراج قال : لما صعد النبي ، وبلغ في السماوات في مكان مرتفع، ومعه جبريل حتى جاوز سدرة المنتهى، فقال له جبريل : إني لم أجاوز هذا الموضع، ولم يؤمر بالمجاوزة أحد هذا الموضع غيرك، فجاوز النبي ﷺ حتى بلغ الموضع الذي شاء الله، فأشار إليه جبريل بأن سلم على ربك، فقال النبي : التحيات الله، والصلوات والطيبات. قال الله تعالى : السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته، فأراد النبي ﷺ أن يكون لأمته حظ في السلام فقال : السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين ، فقال جبريل وأهل السماوات كلهم : أشهد أن لا إله إلا الله، وأشهد أن محمدا عبده ورسوله

‘Ama kwa wale wanaosema kua Maneno haya yamenukuliwa katika Kisa cha Miraj wanasema kua*Wakati Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipofika katika Sidtrat Al Muntaha pamoja na Jibril basi Malaika Jibril akasema; ‘Hakika mimi sijawahi kuvuka zaidi ya sehemu hii, na hakuna alieruhusika kuvuka isipokua wewe’ hivyo *Rasul Allah Allah Salallahu Alayhi wa Salam akavuka na kuendelea hadi alipojaaliwa kufkia na Allah Subhanah wa Ta’ala na kisha Malaika Jibril akamfahamiha Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Slam namna ya Kumusalimia Allah Subhanah wa Ta’ala kwa kusema Tahiyyat Lillahi wa Salawatu wa Tayyibatu* na hivyo*Allah Subhanah wa Ta'ala* nae akajibu kwa kusema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh*. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina*. Na kisha Malaika Jibril akasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu AnNa Muhammadan Rasul Allah.’*

Imam Al Qurtubi amemnukuu tena Imam Abu Layth Al Samarqand ambae amezungumzia juu ya tukio hili tenakatika Kitabu chake Bahr Ul Ulm. Na pia Imam Abu Fidal al Khalwati katika kitabu chake cha Ruh Al Bayyan, kwa kusema;

وروى– أنه عليه السلام عرج من السماء السابعة إلى السدرة على جناح جبريل ، ثم منها على الرفرف ، وهو بساط عظيم . قال الشيخ عبد الوهاب الشعراني : هو نظير المحفة عندنا . ونادى جبريل من خلفه : يا محمد ، إن الله يثنى عليك فاسمع وأطع ولا يهولنك كلامه ، فبدأ عليه السلام بالثناء ، وهو قوله : «التحيات لله والصلوات والطيبات» أي : العبادات القولية والبدنية والمالية ، فقال تعالى : «السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته» . فعمم عليه السلام سلام الحق ، فقال : «السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين» ، فقال جبريل : «أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمدا عبده ورسوله

‘**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipopandishwa katika Mbingu ya saba Katika Usiku wa Miraj na Malaika Jibril hadi katika Sidrat Na kisha kutoka katika Sidtrat hadi katika Rafraf ambalo ni Zulia Tukufu. Na Shaykh Abdul Wahhab Al Sha’arani amesema kuailikua ni kama Kijumba cha mfalme kinachobebwa na watu wanne kwetu sisi. Hivyo Jibril aliita kutoka nyuma yake: Ewe Muhammad, Allah Subahanah wa Ta’ala anakusifu, basi sikiliza na utii, na usiogope kwa maneno yake, kwa hivyo*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akaanza kumsifu *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa kusema: ‘*Tahiyyat Lillahi wa Salawatu wa Tayyibatu* na hivyo*Allah Subhanah wa Ta'ala* nae akajibu kwa kusema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh*. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina*. Na kisha Malaika Jibril akasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu AnNa Muhammadan Rasul Allah.’***

Na anasema Imam Anwar Shah Al Kashmīrī, katika Alʿ Arf Al Shadhi kua:

وذكر بعض الأحناف قال رسول الله – ﷺ – في ليلة الإسراء : «التحيات لله» إلخ ، قال الله تعالى : السلام عليك أيها النبي» إلخ ، قال رسول الله – ﷺ –: «السلام علينا وعلى عباد: الله» إلخ ، ولكني لم أجد سند هذه الرواية ، وذكره في الروض الأنف .

‘Baadhi ya Mahanafi wamesema kuaImenukulia kua wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipopanda Juu mbinguni alikua akimtukuza *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa maneno haya, (*Tahiyyat Lillahi wa Salawatu wa Tayyibatu*) na hivyo*Allah Subhanah wa Ta'ala* nae akajibu kwa kusema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh*. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina*. Na kisha Malaika Jibril akasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu AnNa Muhammadan Rasul Allah.’*

Na pia imenukuliwa na Shaykh Islami Imam Mullah Ali bin Sultan Muhammad Al Qari Al Qarri katika kitabu chake cha *Mirqat Al Miftah kua*

(وأشهد أن محمداً عبده ورسوله) قال ابن الملك : روي أنه ﷺ لما عرج به أثنى على الله تعالى بهذه الكلمات فقال الله تعالى : السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته . فقال عليه السلام : السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين . فقال جبريل : أشهد أن لا إله إلا الله وأشهد أن محمداً عبده ورسوله . ا هـ . وبه يظهر وجه الخطاب، وأنه على حكاية معراجه عليه السلام في آخر الصلاة التي هي معراج المؤمنين.

Nashuhudia kua Muhamamd *Salallahu Alayhi wa Salam* ni Mja na ni Mtume wa *Allah Subhanah wa Ta’ala* . Amesema Ibn Malik kua: Imenukulia kua wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipopanda Juu mbinguni alikua akimtukuza *Allah Subhanah wa Ta’ala* kwa maneno haya, (*Tahiyyat Lillahi wa Salawatu wa Tayyibatu*) na hivyo*Allah Subhanah wa Ta'ala* nae akajibu kwa kusema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh*. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina*. Na kisha Malaika Jibril akasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah.’*Na hii inamaanisha maana ya Tahiyyat kulingan ana tukio hili la kupanda Mbinguni kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na hivyo mwishoni mwa Sala hua nikupandishwakwa Waumini.

Na mbali ya kua Kauli hii ya tukio hili imezungumziwa na wengi miongoni mwa Wanazuoni Maarufu, lakini hata hivyo kuna Wanazuoni wengi pia wenye kupingana na Mtizamo huo, wakiwemo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Wanazuoni wengineo kama Imam Anwar Shah Al Kashmiri, ambae anasema katika kitabu chake cha *Arf Al Shadhi* mlango wa Yaliyotajwa kuhusiana na Tashhud kua:

و (الصلوات) أي الفعلية. (الطيبات) أي المالية، وذكر بعض الأحناف قال رسول الله ﷺ في ليلة الإسراء: «التحيات الله» إلخ، قال الله تعالى : السلام عليك أيها النبي إلخ، قال رسول الله ﷺ: السلام علينا وعلى عباد الله، إلخ، ولكني لم أجد سند هذه الرواية، وذكره في الروض الأنف،

‘Na (Salawaat) yaanikama ilivyo maana halisi ya Salawat kivitendo. (Attayibat) yaani kama ilivyo maana halisi ya Mambo mazuri kiumiliki wa mali, na baadhi ya Hanafi wamesema kuwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika usiku wa Israa alisema: Tahiyyat Allahhivyo *Allah*

Subhanah wa Ta'ala* nae akajibu kwa kusema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh.* Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina.'* lakini mimi sikupata sanad ya upokezaji wake riwaya hii, na imetajwa katika *Al Rawdh Al Anf.'

Na katika Ma'arif Al Sunan Sharh Jami' Al Tirmidhi cha Muhammad Yusuf Al Bannuri katika Mlango wa Sura ya kile kilichotajwa kuhusiana na Tashshahud kua: **'Baadhi ya Mahanafi wamesema kuaImenukulia kua wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipopanda Juu mbinguni alikua akimtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa maneno haya, (*Tahiyyat Lillahi wa Salawatu wa Tayyibatu*) na hivyo*Allah Subhanah wa Ta'ala* nae akajibu kwa kusema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh*. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina*. Na kisha Malaika Jibril akasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah.'***

Na Imesimuliwa na Ali Al Qari kutoka kwa Ibn Abd Al Malik katika 'Al Marqah'. Kisha Al Qari akasema baada ya kuisimulia:'Na kutokana na hili maana ya Tahiyyat inadhihirika, na inatokana na riwaya ya kupaa kwake (*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*) na hivyo mwishoni mwa Salah ambayo ni kupaa kwa (Amali za) Waumini.'

Hivyomwandishi Imam Ali Al Qari amesema: 'Makusudio yake sio kuisoma kama hadithi au riwaya, bali anaisoma akikusudia maneno yake yafikishe maana iliyokusudiwa kama kitendo cha kujenga, kama ilivyoelezwa katika "Al Mujtaba", na kama ilivyosimuliwa na mwandishi wa "Al Bahr" na wengine. Mwenye kusali hua ni mwenye kumsalimu *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua ni humtakia Amani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*yeye mwenyewe na walii wake. Bali yule aliyesema hivyo alimaanisha kwamba maneno haya yalifanywa mwishoni mwa Sala kama ukumbusho wa neema hiyo kubwa, ambayo ni kupaa kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuelekea Mbinguni kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* .

Hivyo Sala yenyewe ni moja kati ya karama za Safari ya Isra ambayoSala nayo hua ni sawa na kupaa kwa Muumini, hivyo ilifaa kuiweka ndani yake kuwa ni mfano wa kuigwa, kisha kuwa ukumbusho wa neema hiyo kubwa iliyomo ndani yake. baraka kubwa. Hivyo basi, kwa usemi wake huo ni kusimamisha salamu za *Allah Subhanah wa Ta'ala* na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kwa maamkizi ya Uislamu ambayo imekuwa kauli mbiu katika Ummah wa Kiislamu, na kwa kuithibitisha, ni ukumbusho wa hilo tukioambalo fahari kubwa sana kwa*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, naAllah Subhanah wa Ta'ala ndiye anayejua zaidi. Imam akasema: Sikupata mnyroro wa upokezaji wa riwaya hizi, isipokuwa amezitaja katika "Al Rawdh Al Anf" pia (2-20) mwanzoni mwa maudhui ya juu ya Adhana ya Sala, lakini kuna tofauti fulani. katika maneno yake'

Rawdh Al Anf ni *Al Rawḍ Al unuf fī šarḥ Al sīra Al Nabawiyya li-Ibn Hišām. wa-maʿahu Al Sīra Al Nabawiyya* ambacho ni kitabu cha Imam Abu Al Qasim na Abu Zayd Abd Al Rahman Ibn Abd Allah Al Suhayli ambae amesema ndani yake kua:

وينضاف إليها في هذا الحديث ذكر الأذان الذي تضمنه حديث البزار مع ما روي أيضا أنه مر وهو على البراق بملائكة قيام وملائكة ركوع وملائكة سجود وملائكة جلوس ، والكل يصلون لله ، فجمعت له هذه الأحوال في صلاته وحين مثل بالمقام الأعلى ودنا فتدلى ، ألهم أن يقول : «التحيات لله» إلى قوله : «الصلوات لله» ، فقالت الملائكة : «السلام عليك أيها النبي ورحمة الله وبركاته» ،

فقال : «السلام علينا وعلى عباد الله الصالحين» ، فقالت الملائكة : «أشهد أن لا إله إلا الله ، وأشهد أن محمدا رسول الله» ، فجمع ذلك له في تشهده .

Kwa kuongezea katika hadithi hii ni kutajwa kwa Adhana, ambao ulijumuishwa katika Hadithi ya Al Bazzar, pamoja na yaliyopokewa pia ni kwamba, wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokuwa juu ya Al Buraq, alipita kwa Malaika waliokua wamesimama, waliokua wamerukuu, waliosujudu, na Malaika waliokaa, na wote walikua wakimuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* , hivyo basi hatua hizi zilizjumuishwa kwa ajili yake katika Salayake, na alipofikia daraja la juu na akakaribia na kushuka, aliongozwa na wahyi kusema: *'Tahiyyat Allahi'*hadi katika kauli: *'Salawatu Allahi'*

Kisha Malaika wakasema *Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh.* Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema *Assalamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihiina.* Na kisha Malaika Jibril akasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah.*'na hivyo akajumuishiwa hayo katika Tashshahud.'

Hivyo wanasema Wanazuoni wanaopingana na mnasabaha huu akiwemo Al Muhaddith Shabbir Ahmad 'Uthmani, Imam Muhammad Yusuf Binnuri, n.kkua **'Kauli hii ya Asili ya Attahiyat kunasibihiana na Safari ya Miraj ni kutokana na Mitizamo yao Wanazuoni husika kutokana na Matukio yaliyotokea ndani ya Safari ya Miraj na hii ni kwa sababu:**

1-Hakuna *(Sanad)*Msururu wa Walionukuu unaoaminika,katika Hadith Sahih wala Dhaif kuhusiana a kauli hizo.

2-Hadith za Miraj Ziko Nyingi sana na hakuna iliyozungumzia tukio hili.

3-Tahiyyat Asilia imetajwa kwenye Hadith Sahih ambazo ni nyingi.

Kama tutakavyoona katika aina ya Visomo vya Tashahud au Tahiyyat kwani Kila Madhhab ina Kisomo chake.

AINA ZA TASHAHUD/TAHIYYAT

❖❖❖

Hivyo miongoni mwa Hadithi zinazokubalika zaidi kuhusiana na Asili ya Attahiyat basi ni ile hadith inayopatikana katika vitabu vya Hadith vya Sahih Bukhari na Sunnan An Nasai ambayo inasema kua:

أَخْبَرَنِي عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ خَالِدٍ الرَّقِّيُّ، قَالَ حَدَّثَنَا حَارِثُ بْنُ عَطِيَّةَ، - وَكَانَ مِنْ زُهَّادِ النَّاسِ - عَنْ هِشَامٍ، عَنْ حَمَّادٍ، عَنْ إِبْرَاهِيمَ، عَنْ عَلْقَمَةَ، عَنِ ابْنِ مَسْعُودٍ، قَالَ كُنَّا إِذَا صَلَّيْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم نَقُولُ السَّلاَمُ عَلَى اللَّهِ السَّلاَمُ عَلَى جِبْرِيلَ السَّلاَمُ عَلَى مِيكَائِيلَ . فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " لاَ تَقُولُوا السَّلاَمُ عَلَى اللَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ السَّلاَمُ وَلَكِنْ قُولُوا التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ

وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لاَ شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ "

‘Amesema Abd Rahman Ibn Khalid Raqqi kua amesema Harith Ibn Aatiyya kua amesema Hisham kua amesema Hamad, kua amesema Ibrahim kua amesema Alqaamah kua amesema Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua:

Tulikua sisi tunaposali na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tukisema: Salaamun aAla Allahi (Salam ziwe juu ya Allah), *Salaamun aAla Jibril*(Salaam ziwe juu ya Jibril),*Salaamun aAla Mikail*(Salam ziwe juu ya Mikail)Hivyo *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* akasema: Msiseme *Salamun aAla Allahi* (Salam ziwe juu ya Allah) kwani kwa Hakika Allah Mwenyewe ndio Salam, bali semeni:*Attahiyatu, Lillahi was Salawatu Wattayyibatu, Asalamu aAlayka Ayyuhan Nabiyyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuhu, Asalamun aAlayna wa Ala Ibadi Illahi Salihin wa Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammadan aAbduhu Wa Rasuluhu(Sahih Muslim)*

***Attahiyat Lillahi* - Heshima zote (Juu ya Allah)**
***Wasalawatu* - Na Sala zote(Juu ya Allah)**
***Wa Tayyibat*- Na Maneno yote Mazuri(Juu ya Allah)**
Asalamu Alayka Ayyuha Nabbiyu* - Salam ziwe juu yako Ewe Nabii(Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam)
***Warahmat Allahi Wabarakatuh* - Na Rehma za Allah na Baraka zake)**
***Asalamu aAlayna* - Salam ziwe juu yetu Sisi(Waislam)**
Wa aAla Aibadi Allahi Salihiina* - Na Waja Wema wa Allah *(Subhanah wa Ta'ala)
***Ashhadu An La Ilaha Illa Allah* - Nashududia kua Hakuna Mungu Ila Allah**
***Wa Ashhadu An Na Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu* - Na Nnashuhudia kua Muhammad*(Salallahu Alayhi wa Salam)* Ni Mja wake na Mtume wake.**

Naam..hii ni Hadith ambayo inaelezea kuhusiana na namna Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walivyokua wakisoma Attahiyat yao hapo kabla ndani ya Sala.Ambapo kama tulivyoelezea kua Attahiyyat kua maana yake ni Kukipaheshima kitu.Na hivyo kutokana na maana hio basi Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakawa Wanamtakia *Salam Allah Subhanah wa Ta'ala*, kisha Malaika Jibril ambae ndie Kiongozi Mkuu wa Malaika na kisha Malaika anaefuatia ambae ni Mikail.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipogundua juu ya hilo basi akawakosoa Masahaba zake Radhi Allahu Anhum.Na akawafundisha Attahiyat bora kabisa na kwa kua Neno Attahiyat liko katika hali ya Wingi wa *Tahiyya* yaani wingi wa Heshima, na hakuna naestahiki zaidi wingi wa Heshima kutoka kwa kiumbe zaidi ya Muumba basi ndio Attahiyat hii ikaanza uthibitisho wa Wingi wa Heshima kua ni wenye kumstahiki*Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee. Na kila Maombi na maneno Mazuri yanàstahiki kua ni kwa ajili ya Allah Tu.

Kisha baada ya hapo Heshima inamuangukia Mbora wa Viumbe ambae ni *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa Kumsalia na kumtakia Salama.Kisha ndio inafuata heshima ya kila Kiumbe anaesimamia heshima hio mbele ya Mola Mtukufu wake na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na kisha inafuata Kuadhimishwa heshima ya Waja wema wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Na kisha ndio inafuatia *Kalimat Al Shahada* yaani Kauli ya kudhibitisha kushuhudia kwa Moyo wa Mhusika kua hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki ila *Allah Subhanah wa Ta'ala* na

kuthibitishia kua Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam kua* ni Mja wa *Allah Subahanh wa Taala* na pia ni Mtume wake.

Naam..hio ni kwa ufupi kuhusiana na Hadith hii ambayo pia inatuthibitishia Darja ya Muumini kutokana na kumheshimu Mola wake na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* na kujiheshimisha kwake katika Kutii maamrisho yake ikiwemo kumuabudia Mola wake Katika Sala yake.

Kwani kama tumeisoma vizuri Tahiyyat hii basi tutakua tumeona kua iko tofauti na Tahiyyat tunazosoma Sisi katika Sala zetu, hususan katika Maneno yasemayo At Tahiyyat Lillahi Wa Salaawatu wa Tayyibatu.

Na hii ni kwa sababu hii ni At Tahiyyat ambayo inatumiwa na Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa. Na kama tulivyosema hapo awali kua Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa ni Fiqh inayotokana na Msingi wa Fiqh wa Sahaba Mwanazuoni Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* kulingana na Mtizamo wa Nyingi miongoni mwa Hadith alizopokea yeye kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na hivyo haishangazi kuona kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa WametumiaAt Tahiyyat hii kutoka kwake kama vile wanavyotumia mitizamo myengine kutoka kwake.

Kwani pia kama nilivyosema hapo awali kua Kila Madhhab yanatofautiana katika Kisomo cha Tahiyyat yao kama tutakavyoona baada ya kuona Tahhiyat ya Abd Allah Ibn Masud Radhi Allahu Anhu, lakini hata hivyo nataka tufahamiane kua tofauti baina ya Tahiyyat hua ni katika Maneno Matatu hadi Manne mwanzo tu ambayo ni yenye kumaanisha Kuonesha Heshima Mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kumsifu kulingana na Sifa zake Tukufu.

Na hivyo hakuna tofauti nyengineyo zaidi, hivyo basi Tahhiyat zote ni sawa na Mtu anaweza kusoma aitakayo kwani zoteNi zenye kutumika kutokana na Vithibitisho vya Hadith Sahih za *Rasul Allah Sallahu Alayhi wa Salam* kulingana na namna alivyowafundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum*. Ila tofauti ya Matumizi hua ni kutokana na Mitizamo ya Wanazuoni wa Madhhab husika kulingana Nguvu za Hoja za Vithibitisho vyenye kuaminika na kukubalika zaidi kwa Ilm ya Sahaba husika na Usahih wa upokewaji wa Hadith husika hadi kufika mbele ya Wanazuoni husika.

Kwani kuna Hadithi isemayo kua:

أَخْبَرَنَا قُتَيْبَةُ، قَالَ حَدَّثَنَا عَبْثَرٌ، عَنِ الأَعْمَشِ، عَنْ أَبِي إِسْحَاقَ، عَنْ أَبِي الأَحْوَصِ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ، قَالَ عَلَّمَنَا رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم التَّشَهُّدَ فِي الصَّلاَةِ وَالتَّشَهُّدَ فِي الْحَاجَةِ فَأَمَّا التَّشَهُّدُ فِي الصَّلاَةِ " التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ " . إِلَى آخِرِ التَّشَهُّدِ

Amesema Qutaybah kua amesema Abthar kua amesema Al Amash kua amesema Abi Is-haq kua amesema Abi Al Ahwas kua amesema Abdi Allahi *Radhi Allahu Anhu* kua*: Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitufundisha Sisi Tashshahud ya Sala na Tashshahud ya Al Haja na Tahiyyat ya Sala ni:*At Tahiyyatu Lillahi wa Salawatu sa Tayyibatu As Salamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, As Salamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihina, Ashhadu An*

Lailaha Ila Allah wa Ashhadu Ana Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu hadi mwisho wa Tahiyyat.'*(Sunan An Nasai)*.

Ambapo Imam Ibn Majah pia anahadithi hii ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* lakini yenye maneno yasemayo kua:

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ قَالَ أُوتِيَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ جَوَامِعَ الْخَيْرِ وَخَوَاتِمَهُ فَعَلَّمَنَا خُطْبَةَ الصَّلَاةِ وَخُطْبَةَ الْحَاجَةِ خُطْبَةُ الصَّلَاةِ التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ وَخُطْبَةُ الْحَاجَةِ أَنْ الْحَمْدُ لِلَّهِ نَحْمَدُهُ وَنَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُضْلِلْ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ ثُمَّ تَصِلُ خُطْبَتَكَ بِثَلَاثِ آيَاتٍ مِنْ كِتَابِ اللَّهِ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ يُطِعْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا

Kutoka kwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*ambae amesema kua*: Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitufundisha Sisi Khutba ya Sala na Khutba ya Al Haja na Tahiyyat ya Sala ni:*At Tahiyyatu Lillahi wa Salawatu wa Tayyibatu As Salamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, As Salamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihina, Ashhadu An Lailaha Ila Allah wa Ashhadu Ana Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu hadi mwisho wa Tahiyyat.*

Na Khutba ya Haja ni kusema:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

الْحَمْدُ لِلَّهِ نَحْمَدُهُ وَنَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ وَمَنْ يُضْلِلْ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

قال الله تعالى يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ

وقال الله وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا

وقال الله اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ يُطِعْ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا

Shukrani zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta'ala* , Tunamtukuza na kumuomba msaada wake, na kumuomba Msamaha wake. Tunaomba hifadhi kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana naMaovu ya Nafsi zetu na maovu ya Amali zetu. Anaeongozwa na Allah, basi hakuna atakaempotosha na atakaepotoshwa na Allah basi hakuna atakaemuongoa, Nashuhudia kua hakuna Mola anaestahiki kuabudiwa kwa Haki isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee asiekua na mshirika na Muhammad ni Mja wake na Mtume wake. Na kisha endelea na Khutba yako kwa kutumia aya tatu kutoka katika Kitabu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* zisemazo:

﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلاَ تَمُوتُنَّ إِلاَّ وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha haqqa tuqatihi wala tamootunna illa waantum muslimoona *(Surat Al Imran 3:102)*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Muogopeni Allah (kwa kutekeleza maamrisho yake na kuachana na makatazo yake) kama anavyostahiki kuogopewa. [Mtiini, mshukuruni na daima mkumbukeni], na msife isipokua mkiwa katika hali ya kua ni Waislam.***

﴿يَأَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُواْ رَبَّكُمُ الَّذِى خَلَقَكُمْ مِنْ نَّفْسٍ وَحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالاً كَثِيراً وَنِسَآءً وَاتَّقُواْ اللَّهَ الَّذِى تَسَآءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيباً﴾

Ya ayyuha alnnasu ittaqoo rabbakumu alladhi khalaqakum min Nafsin wahidatin wakhalaqa minha zawjaha wabaththa minhuma rijalan kathiran wanisaan waittaqoo Allaha alladhii tasaaloona bihi waAl arhama inna Allaha kana AAalaykum raqeeban *(Surat An Nisaa 4:1)*

Tafsiri: ***Enyi Watu! Mcheni Mola wenu aliekuumbeni kutokana na Nafsi moja (Adam), na kutokana nae (Adam) akamuumba mke wake (Hawwa), na kutokana nao (Adam na Hawa) akawaumba Wanaume na Wanawake wengi na muogopeni Allah ambae ana haki juu yenu, na msivunje udugu, kwani kwa Hakika Allah ni mwenye uangalifu mkubwa juu yenu.***

﴿يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُواْ اتَّقُواْ اللَّهَ وَقُولُواْ قَوْلاً سَدِيداً ۞ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَلَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَن يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزاً عَظِيماً﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo ittaqoo Allaha waqooloo qawlan sadeedan, Yuslih lakum aAAmalakum wayaghfir lakum dhunoobakum waman yutiAAi Allaha warasoolahu faqad faza fawzan AAadhiman*(Al Ahzab 33:70-71)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini! mcheni na muogopeni Allah, na (daima) semeni kauli za ukweli ulionyooka, atakuongozeni kufanya mema na kukusameheni dhambi zenu. Na kwa hakika yeyote yule ambae anaemtii Allah na Mtume wake (Salallahu Aa'layhi wa Salam) basi atakua ni miongoni mwa waliofuzu kwa Darja kubwa.'*** *(Sunan Ibn Majah).*

Ambapo naunaweza kumalizia na maneno ya hadithi ifuatayo

إِنَّ أَصْدَقَ الْحَدِيثِ كِتَابُ اللَّهِ وَأَحْسَنَ الْهَدْيِ هَدْيُ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَشَرُّ الْأُمُورِ مُحْدَثَاتُهَا وَكُلُّ مُحْدَثَةٍ بِدْعَةٌ وَكُلُّ بِدْعَةٍ ضَلَالَةٌ وَكُلُّ ضَلَالَةٍ فِي النَّارِ

أَمَّا بَعْدُ ...

Maneno ya kweli kabisa ni Kitabu cha Allah Subhanah wa wa Ta'ala, na uwongofu ulio bora zaidi ni uongofu wa Muhammad, Salallahu Alayhi wa Salam. Mambo mabaya zaidi ni yale yaliyozuliwa, na kila jambo lililozushwa upya hua ni uzushi, na kila uzushi ni upotofu, na kila upotofu uko Motoni.

Ambapo kuhusiana na Hadith mbili hizi za Tashahud au Tahiyyat basi tunaona kua ndani yake mmetajwa Tashahud mbili, ya Sala na ya Haja na kwa upande wa hadith ya pili mmetajwa Khutba mbili ya Sala na ya Haja.

Na ndani yake tunaona kua kuhusiana na Tashahud na Khutba ya Sala kua haikumaanisha kitu chengine chochote isipokua ni Tahiyat. Hivyo kuhusiana na Tashshahud au Tahiyyat au Khutba ya Haja, ambayo Hadith imethibitisha kua Maneno yenye kujumuisha shukran, kutuza na maombi ya dua kama inavyosema Hadith na kumalizia na Aya tatu zenye kusisitiza jukumu la Tawhid na Ucha Mungu zilizomo ndani yake na limetumika neno Haja kwa sababu utumiwaji wake hua unajumuisha takriban katika uanzishaji wa kila Jambo jema ambalo Muislam anataka kulifanya kwa manufaa ya Jamii ya Kiislam, kwani ni zenye kuhimiza Kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kila kitu Tukisemacho na tukifanyacho, hivyo hua ni Sunna inayopendekezwa kusoma Khutba ya Haja au Tashahud ya Haja au Tahiyyat ya Haja katika kila Mwanzoni mwa Jambo jema kama vile Kusomesha Darsa, Kuandika Vitabu vya Ilm ya Dini ya Kiislam, Kutoa Mawaidha, Kusoma Khutba za Sala za Ijumaa, Sala za Idd, Kusoma Khutba ya Kuozesha na kwenye Mijumuiko inayojumuisha Haja mbali mbali ya Kislam.

Kwani anasema Imam Al Tayalisi kua: **'Shu'bah alimuuliza Imam Abu Is-haq kuhusiana na Khutba ya Haja kwa kusema: 'Jee hii Khutba ni katika Khutba ya Ndoa au na katika mambo mengine pia?' ambapo Imam Abu I-haq akasema: 'La sikatika Khutba ya Ndoa tu bali katika kila Haja.''**

Na IngawaAl Hafidh Al Faqih Imam Muhammad Ibn Alan Al Sadiqi Al Shafii kua:**'Miongoni mwao Khutba za Haja ni pamoja na Khutba ya Sala ya Ijumaa na Sala za Idd na mambo kama hayo kwa sababu haya ndio mambo ya kawaida katika wakati huo tofauti na Khutba za kama kwenye Uandishi wa vitabu, At Tirmidhii hakuiandika katika vitabuvyake vya Jamii Tirmidhii na Sharmail At Tirmidhii, na AbuDaud pia ambapo wao ndio Wanazuoni wa ukusanyaji wa Hadith, hivyo vitendo vya vinaonesha kua Khutba ya Haja inahusiana na mambo maalum kama yaliyotajwa'** *(Futuh Rabbaniyah)*

Lakini Imam Mulla Ali Al Qari basi yeye anasema kua: **'Kwa kua wengi miongoni mwa Wakusanyaji wa Hadith hawakuifanyia kazi maana inayoonekana wazi ya Hadithi hii (Kila Khutba isiyojumuisha ndani yake Tashahud basi hua ni kama iliyokatwa Mikono) na hivyo hii inamaanisha kua maana yake hua haikusudiwi na hivyo huweza kutafsiriwa katika Tafsir tofauti**

kimaana. Ambapo jambo lililowazi kabisa juu ya Hadithi hii ni kutaka ifahamike kua inahusiana na yale mambo yaliyokua yakifanyika katika nyakati hizo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kama katika Khutba za siku ya Ijumaa, Sala za Idd na matukio ya siku nyenginezo kwa sababu ukusanyaji ulifanywa baada yake.'*(Jamii Wasail Sharh Sharmail)***

Tunarudi katika Tashahud ya Sala na kuona kua amesema pia Imam Ibn Majah kupitia katika Hadith ya Imam Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahuu Anhu* kua;

حَدَّثَنَا جَمِيلُ بْنُ الْحَسَنِ، حَدَّثَنَا عَبْدُ الأَعْلَى، حَدَّثَنَا سَعِيدٌ، عَنْ قَتَادَةَ، ح وَحَدَّثَنَا عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ عُمَرَ، حَدَّثَنَا ابْنُ أَبِي عَدِيٍّ، حَدَّثَنَا سَعِيدُ بْنُ أَبِي عَرُوبَةَ، وَهِشَامُ بْنُ أَبِي عَبْدِ اللَّهِ، عَنْ قَتَادَةَ، . وَهَذَا حَدِيثُ عَبْدِ الرَّحْمَنِ عَنْ يُونُسَ بْنِ جُبَيْرٍ، عَنْ حِطَّانَ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، عَنْ أَبِي مُوسَى الأَشْعَرِيِّ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ خَطَبَنَا وَبَيَّنَ لَنَا سُنَّتَنَا وَعَلَّمَنَا صَلاَتَنَا، فَقَالَ " إِذَا صَلَّيْتُمْ، فَكَانَ عِنْدَ الْقَعْدَةِ، فَلْيَكُنْ مِنْ أَوَّلِ قَوْلِ أَحَدِكُمُ التَّحِيَّاتُ الطَّيِّبَاتُ الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، سَبْعُ كَلِمَاتٍ هُنَّ تَحِيَّةُ الصَّلاَةِ " .

AmesemaJamil Ibn Hasan kua amesema Abd Al Aala kua amesema Said kua amesema Qatadah kua amesema Abd Raan Ibn Umar kua amesema Ibn Abi Aadiyi kua amesema Said Ibn Abi Aaruba kua amesema Hisham Ibn Abd Allahi kua amesema Qatadah kua amesema Abd Raan alieambiwa na Yunus Ibn Jubayr kua amesema Khitani Ibn Abdillahi Kua amesema Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituhutubia na kutuelezea Sunna kwa ajili yetu, akatufundisha Sala zetu kwa kusema:Mnaposali, katika wakati wa kikao cha kukaa kitako cha Sala basi kitu cha mwanzo mnachotakiwa kusema ni: *At Tahiyyat At Tayyibatu As Salawatu, Assalamu Alayka Ayyuha Nnabiyu wa Rahmat Allahi wabarakatuhAs Salamu Alayna wa Ala Ibadi Allahi Salihiina, Ashhadu An Lailaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu, Hizi ni Kauli Saba za maneno ya Tahiyyat ya Sala (*Sunan Ibn Majah)**

Ambapo kwa upande wa Imam An Nasai yeye ameinukuu hadithi hii kwa kusema:

أَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ مَسْعُودٍ، قَالَ حَدَّثَنَا خَالِدٌ، قَالَ حَدَّثَنَا سَعِيدٌ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ يُونُسَ بْنِ جُبَيْرٍ، عَنْ حِطَّانَ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، أَنَّهُ حَدَّثَهُ أَنَّهُ، سَمِعَ أَبَا مُوسَى، قَالَ إِنَّ نَبِيَّ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم خَطَبَنَا وَبَيَّنَ لَنَا سُنَّتَنَا وَعَلَّمَنَا صَلاَتَنَا فَقَالَ " إِذَا صَلَّيْتُمْ فَأَقِيمُوا صُفُوفَكُمْ ثُمَّ لْيَؤُمَّكُمْ أَحَدُكُمْ فَإِذَا كَبَّرَ الإِمَامُ فَقُولُوا آمِينَ يُجِبْكُمُ اللَّهُ وَإِذَا كَبَّرَ وَرَكَعَ فَكَبِّرُوا { غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلاَ الضَّالِّينَ }فَكَبِّرُوا وَإِذَا قَرَأَ وَارْكَعُوا فَإِنَّ الإِمَامَ يَرْكَعُ قَبْلَكُمْ وَيَرْفَعُ قَبْلَكُمْ " . قَالَ نَبِيُّ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " فَتِلْكَ بِتِلْكَ وَإِذَا قَالَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ فَقُولُوا اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ يَسْمَعِ اللَّهُ لَكُمْ فَإِنَّ اللَّهَ قَالَ عَلَى لِسَانِ نَبِيِّهِ

صلى الله عليه وسلم سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ فَإِذَا كَبَّرَ وَسَجَدَ فَكَبِّرُو وَاسْجُدُوا فَإِنَّ الإِمَامَ يَسْجُدُ قَبْلَكُمْ وَيَرْفَعُ قَبْلَكُمْ قَالَ نَبِيُّ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " فَتِلْكَ بِتِلْكَ فَإِذَا كَانَ عِنْدَ الْقَعْدَةِ فَلْيَكُنْ مِنْ أَوَّلِ قَوْلِ أَحَدِكُمُ التَّحِيَّاتُ الطَّيِّبَاتُ الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ سَلاَمٌ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ سَلاَمٌ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ سَبْعَ كَلِمَاتٍ وَهِيَ تَحِيَّةُ الصَّلاَةِ "

Amesema Ismail Ibn Masud kua amesema Khalid kua amesema Said kua amesema Qatadah kua amesema Yunus Ibn Jubayr kua mesema Hittan Ibn Abd Allah kua amemseikia Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* akisema: *'Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alituhutubia sisi Na kisha akatufundisha sisi Sunna zetu na Sala zetu huku akisema: 'Wakati mnaposali, basi nyoosheni Safu zenu, na mchagueni mmoja wenu akuongozeni ndani ya Sala yenu, Imam anaposema Takbr, basi nanyi semeni Takbir, anaposoma; '*Ghayril Al maghdhuubi Aalayhim wa Dhaaliin*' basi itikieni Amiin''na Allah atakujibuni, Imam atakasema Takbir na kurukuu basi na nyinyi semeni Takbir na Rukuuni, Imam anarukuu na anasimama mbele yenu kabla yenu.'

'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema; 'Hivyo kwa hivyo na atakaposema *'Sami Allahu Liman Hamida*' basi semeni '*AllahumaRabbana Laka Al Hamd' na Allah atakusikieni kwani Allah hua ni mwenye kusema kupitia katika Midomo ya Mtume wake.'* Na Imam anaposema Takbir na kusjudu basi nanyi semeni Takbir na Sujuduni, Imam anasujudu mbele yenu kabla yenu na kukaa mbele yenu kabla yenu, Hivyo hivyo, na anapokaa kitako basi jambo la kwanza kwa kila mmoja wenu kusema liwe ni: *'At-tahiyaatut-tayyibatus-salawatuLillah, salamun 'alayka ayyuhanabiyyu wa rahmatullahi wa barakatuhu, salamun 'alayna wa 'ala 'ibadillahis-salihin, ashhadu an la ilaha ill-Allah wa ashhadu anna Muhammadan 'abduhu wa rasuluh''(Imam An Nasai)

Naam, katika Hadith hii ya Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* yenye kudhihirisha Kauli 7 za *Tahiyyat* tunaona kua maneno ni yale yale ila tofauti ni katika mpangilio wa bain ya neno la pili na la tatu kwani hii imeanza na neno *Tayyibat* kisha ndio *As Salawat.*

Kwa maana hio basi kisomo hiki cha Tahiyyat ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahi Anhu* ni aina ya kwanza ya *Tahiyyat* au *Tashahhud* ambapo aina ya pili ni hii ya Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu.* Ambapo pia kuna *Tahiyyat* ya hadith ya *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua:

حَدَّثَنَا قُتَيْبَةُ، حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ، عَنْ سَعِيدِ بْنِ جُبَيْرٍ، وَطَاوُسٍ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ، قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يُعَلِّمُنَا التَّشَهُّدَ كَمَا يُعَلِّمُنَا الْقُرْآنَ فَكَانَ يَقُولُ " التَّحِيَّاتُ الْمُبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ الطَّيِّبَاتُ لِلَّهِ سَلاَمٌ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ سَلاَمٌ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ "

قَالَ أَبُو عِيسَى حَدِيثُ ابْنِ عَبَّاسٍ حَدِيثٌ حَسَنٌ غَرِيبٌ صَحِيحٌ . وَقَدْ رَوَى عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ حُمَيْدٍ الرُّؤَاسِيُّ هَذَا الْحَدِيثَ عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ نَحْوَ حَدِيثِ اللَّيْثِ بْنِ سَعْدٍ . وَرَوَى أَيْمَنُ بْنُ نَابِلٍ الْمَكِّيُّ هَذَا الْحَدِيثَ عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ عَنْ جَابِرٍ وَهُوَ غَيْرُ مَحْفُوظٍ . وَذَهَبَ الشَّافِعِيُّ إِلَى حَدِيثِ ابْنِ عَبَّاسٍ فِي التَّشَهُّدِ .

Amesema Qutayba kua amesema Al Layth Ibn Saad kua amesema Abi Zubayr kua amesema Said Ibn Jubayr kua amesema Tawus kua amesema AbdAllah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitufundisha sisi *Tahiyyat* kama vile anavyotufundisha kusoma Qur'an na alikua akisema:

At Tahiyyatu, Al Mubarakatuh, As Salawatu Al Tayyibatu Lillahi Salamu Alayka Ayyuha Nnabiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, Asalamu Alayna wa Aala Aibadi Allahi Salihina, Ashhadu An Lailaha Illa Allah wa Ashhadu AnNa Muhammadan Rasul Allah.*(Sahih Muslim, Sunnan Abu Daud, Sunan At Tirmidhii, Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo amesema Imam Abu Isa Muhammad Ibn Isa At Tirmidhii kuhusiana na Hadith hii ya *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*kua: **'Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas*Radhi Allahu Anhu* ni Sahih Hadith, Hasan Hadith na ni Hadith ngeni, ambapo Abd Rahman Ibn Humayd Al Ruasi ameinukuu Hadith hii Kutokea kwa Abu Al Zubayr ambayo nayo ina maneno kama ya hadith Al Layth Ibn Saad. Na Ayman Ibn Makki pia ameinukuu Hadith hii kutokea kwa Abu Zubayr kupitia kwa Jabir, lakini hata hivyo haikuwahi kuhifadhiwa Hivyo Imam Al Shafii ameichukua Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na Kuitumia katika *Tashshahud.*'**

Kwa hivyo*Tahiyyat* iliyonukuliwa katika Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ni aina ya tatu ya *Tashahhud*,na ndio *Tahiyyat* ya Madhhab ya Imam Al Shafii kama alivyosema Imam At Tirmidhii. Na kwa upande mwengine basi kuna Hadith ya Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua:

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ الأَعْلَى، قَالَ حَدَّثَنَا الْمُعْتَمِرُ، قَالَ سَمِعْتُ أَيْمَنَ، - وَهُوَ ابْنُ نَابِلٍ - يَقُولُ حَدَّثَنِي أَبُو الزُّبَيْرِ، عَنْ جَابِرٍ، قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يُعَلِّمُنَا التَّشَهُّدَ كَمَا يُعَلِّمُنَا السُّورَةَ مِنَ الْقُرْآنِ " بِسْمِ اللَّهِ وَبِاللَّهِ التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ السَّلاَمُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلاَمُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ أَسْأَلُ اللَّهَ الْجَنَّةَ وَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ النَّارِ" .

Amesema Muhammad Ibn Abd Al Aalakua amesema Muutamir kua amesema Nimemsikia mimi Aymaan ambae ni Ibn Nabil akisema kua amesema Abu Zubayr kua amesema *Jabir Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitufundisha sisi Tashahud kama vile alivyokua akitufundisha Sura kutoka kwenye Qur'an kwa kusema: '*Bismi Allahi wa Bi Allahi At Tahiyyat lillahi Wa Salawat wa Tayyibat Asalamu aAlayka Ayyuhan Nabiyyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuhu, Asalamun aAlayna wa Ala Ibadi Illahi Salihin wa Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa*

Ashhadu Anna Muhammadan aAbduhu Wa Rasuluhu As Al Allaha Al Jannah wa Aaudhu bi Allahi Minna Nnar.'*(Imam An Nasai)*

Na ingawa Imam Al Hakim amesema kuhusiana na Hadith hii kua ni Sahih, lakini kwa upande wa Imam Bukhari, Imam At Tirmidhi, Imam Al Bayhaqi na Imam An Nasai basi wao wanasema kua**: 'Hii ni hadith dhaif kwa sababu, alieinukuu ni mtu ambae amefanyakosa katika kuinukuu kwake, na hii kwa sababu imethibitishwa katika Hadith ya Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu*ambae amesema kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

أَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ مَسْعُودٍ، قَالَ حَدَّثَنَا خَالِدٌ، قَالَ حَدَّثَنَا سَعِيدٌ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ يُونُسَ بْنِ جُبَيْرٍ، عَنْ حِطَّانَ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، أَنَّهُ حَدَّثَهُ أَنَّهُ، سَمِعَ أَبَا مُوسَى، قَالَ إِنَّ نَبِيَّ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم خَطَبَنَا وَبَيَّنَ لَنَا سُنَّتَنَا وَعَلَّمَنَا صَلاَتَنَا فَقَالَ " إِذَا صَلَّيْتُمْ فَأَقِيمُوا صُفُوفَكُمْ ثُمَّ لْيَؤُمَّكُمْ أَحَدُكُمْ فَإِذَا كَبَّرَ الإِمَامُ فَقُولُوا آمِينَ يُجِبْكُمُ اللَّهُ وَإِذَا كَبَّرَ وَرَكَعَ { غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلاَ الضَّالِّينَ }فَكَبِّرُوا وَإِذَا قَرَأَ فَكَبِّرُوا وَارْكَعُوا فَإِنَّ الإِمَامَ يَرْكَعُ قَبْلَكُمْ وَيَرْفَعُ قَبْلَكُمْ " . قَالَ نَبِيُّ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " فَتِلْكَ بِتِلْكَ وَإِذَا قَالَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ فَقُولُوا اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَلَكَ الْحَمْدُ يَسْمَعِ اللَّهُ لَكُمْ فَإِنَّ اللَّهَ قَالَ عَلَى لِسَانِ نَبِيِّهِ صلى الله عليه وسلم سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ فَإِذَا كَبَّرَ وَسَجَدَ فَكَبِّرُو وَاسْجُدُوا فَإِنَّ الإِمَامَ يَسْجُدُ قَبْلَكُمْ وَيَرْفَعُ قَبْلَكُمْ قَالَ نَبِيُّ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " فَتِلْكَ بِتِلْكَ فَإِذَا كَانَ عِنْدَ الْقَعْدَةِ فَلْيَكُنْ مِنْ أَوَّلِ قَوْلِ أَحَدِكُمُ التَّحِيَّاتُ الطَّيِّبَاتُ الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ سَلاَمٌ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ سَلاَمٌ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ سَبْعَ كَلِمَاتٍ وَهِيَ تَحِيَّةُ الصَّلاَةِ "

Amesema Ismail Ibn Masud kua amesema Khalid kua amesema Said kua amesema Qatadah kua amesema Yunus Ibn Jubayr kua mesema Hittan Ibn Abd Allah kua amemseikia Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* akisema: '*Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alituhutubia sisi Na kisha akatufundisha sisi Sunna zetu na Sala zetu huku akisema: 'Wakati mnaposali, basi nyoosheni Safu zenu, na mchagueni mmoja wenu akuongozeni ndani ya Sala yenu, Imam anaposema Takbr, basi nanyi semeni Takbir, anaposoma; '*Ghayril Al maghdhuubi Aalayhim wa Dhaaliin*' basi itikieni Amiin'' na Allah atakujibuni, Imam atakasema Takbir na kurukuu basi na nyinyi semeni Takbir na Rukuuni, Imam anarukuu na anasimama mbele yenu kabla yenu.'

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema; 'Hivyo kwa hivyo na atakaposema '*Sami Allahu Liman Hamida*' basi semeni '*AllahumaRabbana Laka Al Hamd' na Allah atakusikieni kwani Allah hua ni mwenye kusema kupitia katika Midomo ya Mtume wake.'* Na Imam anaposema Takbir na kusjudu basi nanyi semeni Takbir na Sujuduni, Imam anasujudu mbele yenu kabla yenu na kukaa mbele yenu kabla yenu, Hivyo hivyo, na anapokaa kitako basi jambo la kwanza kwa kila mmoja wenu kusema liwe ni: '*At-tahiyaatut-tayyibatus-salawatuLillah, salamun 'alayka ayyuhanabiyyu wa rahmatullahi wa barakatuhu, salamun 'alayna wa 'ala 'ibadillahis-salihin,*

ashhadu an la ilaha ill-Allah wa ashhadu anna Muhammadan 'abduhu wa rasuluh''*(Imam An Nasai, Imam Abd Razaq)*

Hivyo Maneno *Bismi Allahi* ni maneno yaliyoongezwa, kwani *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* hakusema hivyo, kama ilivyosemwa katika Al Mudawwana kua: 'Malik hakua ni mwenye kutaja Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwanzo mwa Tahiyyat, yaani hakuitaja katika Sahih Hadith hata moja, ambapo hatahivyo hii haipingani naukweli wa kua aliinukuu hadithi hii kutoka kwa Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu.'*

Kwani katika Kitabu cha Hadith cha Imam Malik kiitwacho Muwwata Imam Malik kuna Hadith ya Tahiyyat isemayo:

حَدَّثَنِي يَحْيَى ، عَنْ مَالِكٍ ، عَنِ ابْنِ شِهَابٍ ، عَنْ عُرْوَةَ بْنِ الزُّبَيْرِ ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَبْدٍ الْقَارِيِّ ، أَنَّهُ سَمِعَ عُمَرَ بْنَ الْخَطَّابِ وَهُوَ عَلَى الْمِنْبَرِ يُعَلِّمُ النَّاسَ التَّشَهُّدَ ، يَقُولُ : قُولُوا : التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ ، الزَّاكِيَاتُ لِلَّهِ ، الطَّيِّبَاتُ الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ . وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Amesema Yahya kutoka kwa Malik kutoka Ibn Shihab kutoka kwa Urwa Ibn Zubayr kutoka kwa Abd Rahman Ibn Abd Al Qari ambae amesema kua: Amemsikia Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* wakati akiwasomesha Watu Tahiyyat wakati kwenye Mimbar akisema kua: Semeni*Attahiyat lillahi, Az Zakiyyat Lillahi At Tayyibatu wa Salawatu lillahi Asalamu aAlayka Ayyuhan Nabiyyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuhu, Asalamun aAlayna wa Ala Ibadi Illahi Salihin wa Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammadan aAbduhu Wa Rasuluhu**(Muwata Imam Malik)***

Naam..hii ni aina ya tano ya Tahiyyat ambayo ni Tahiyyat inayopendekezwa zaid na Kusomwa na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik. Na tunapoiangalia Hadith hizi basi tunaona kua zimetoka kwa *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* moja kwa moja,katika kuwasomesha kwake Waislam namna ya kusoma At Tahiyyat.Na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik ndio watu pekee wenye kuisoma Tahiyyat hii.

Hivyo basi nasi tuwaangalie wanasemaje wao wenyewe kuhusiana nayo, yaani kwanini wakawa wanaitumia *Tashahhud* hii.Ambapo nao wanasema kua Hadith hii imenukuliwa na Malik kutoka kwa Ibn Shihab kupitia kwa Urwa Ibn Al Zubayr kupitia kwa Al Qari Abd Rahman Ibn Abd ambapo kwanza Sanad nzima ya Hadith hii ni wenye Maimam wenye kuaminika kutokana na Ucha Mungu wao.

Na kwa upande wa Abd Rahman Ibn Abd ni mwenye kutokakatika Kabila la Khuzaimah Ibn Mudrika Al Madani alikua ni Msaidizi wa usimamizi wa Mali za Bayt ul Mal katika wakati wa Utawala wa *Mamlaka ya Amir ul Muuminin* Umar Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu.* Ambapo kwa upande wa Imam Al Ajli basi anasema kua Al Qari Abd Rahman Ibn Abd alikua ni Mtu mwenye Kuaminika miongoni mwa Ta'biina na alifariki mnamo mwaka 88 Al Hijr.

Na Imetajwa katika *Kitab Al Istidhkar li Madhhab Ulama Al Amsar Fi Ma Tadamanahu Al Muwwata min Maa'ani wa al Ray wa Al Athar* cha Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki kua: '**Alichokinuu Malik kutoka kwa Umar Ibn Al Khattab, na pia**

kutoka kwa Mtoto wake na kwa Aisha *Radhi Allahu Anhum* basi vyote hua ni vyenye kutokea kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kwani hii inajulikana wazi kua haitokani na Mtizamo wao mtupu, kwani kama ingekua ni mtizamo mtupu basi Ukumbusho wake usingekumbushwa.Na mbali ya Malik kunukuu kutoka kwa Umar kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* lakini pia kuna na wengine walionukuu.'

'Na Umar Ibn Al Khattabu *Radhi Allahu Anhu* alikua akiisomesha Tahiyyat hii kwenye Mimbar mbele ya Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na hakuna aliepinga wala kuikataa. Na hii inamaanisha kua Tahiyyat hii ndio bora zaidi kuliko nyanginezo na ilikua ikifuatwa na kusomwa. Na Imam Ibn Mardawayh ameinukuu hadith hii kwenye Kitabu chake na kusema kua ni Hadith yenye sifa ya kua ni Marfuu.'

'Hivyo Uthibitisho wa Hadith hii yenye kukubalika kwa Imam Malik hadi akafuata Mtizamo wa At Tahiyyat ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*Kwani ni wenye kukubalika kutokana na Nukuu Mutawwattir nyingi zinazoungana mkono na hii ni kwa sababu Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* aliisomesha kwenye Mimbar mbele ya Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na Maimam wa Waislam bila kupingwa.'*(Al Istidhkar)***

Kwani katika Kitabu cha Hadith cha Imam Malik kiitwacho Muwwata Imam Malik kuna hadith nyengine pia isemayo:

وَحَدَّثَنِي عَنْ مَالِكٍ عَنْ نَافِعٍ أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ عُمَرَ كَانَ يَتَشَهَّدُ فَيَقُولُ: بِسْمِ اللَّهِ، التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ، الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ، الزَّاكِيَاتُ لِلَّهِ، السَّلَامُ عَلَى النَّبِيِّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ، شَهِدْتُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، شَهِدْتُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، يَقُولُ هَذَا فِي الرَّكْعَتَيْنِ الْأُولَيَيْنِ. وَيَدْعُو، إِذَا قَضَى تَشَهُّدَهُ، بِمَا بَدَا لَهُ.

فَإِذَا جَلَسَ فِي آخِرِ صَلَاتِهِ، تَشَهَّدَ كَذَلِكَ أَيْضًا، إِلَّا أَنَّهُ يُقَدِّمُ التَّشَهُّدَ، ثُمَّ يَدْعُو بِمَا بَدَا لَهُ. فَإِذَا قَضَى تَشَهُّدَهُ، وَأَرَادَ أَنْ يُسَلِّمَ، قَالَ: السَّلَامُ عَلَى النَّبِيِّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكُمْ عَنْ يَمِينِهِ، ثُمَّ يَرُدُّ عَلَى الْإِمَامِ فَإِنْ سَلَّمَ عَلَيْهِ أَحَدٌ عَنْ يَسَارِهِ، رَدَّ عَلَيْهِ

Na Amesema Malik kua amesema Nafii kua Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua kila anaposoma Attahiyat husoma kwa kusema:

'Bismi Allahi, Attahiyat lillahi As Salawatu Lillahi, Az Zakiyyat Lillahi, Asalamu aAlayka Ayyuhan Nabiyyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuhu, Asalamun aAlayna wa Ala Ibadi Illahi Salihina.Shahidtu An La Ilaha Illa Allah, Shahidtu Anna Muhammadan aAbduhu Wa Rasuluhu.'

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akisema hivyo katika Tahiyyat yake ya kwanza. Na alikua anapokaa katika Rakaa ya mwisho ya Sala yake alikua akisoma tena hivyo hivyo katika Tahiyyat yake ya pili isipokua huanza na Tahiyyat hio na kisha humalizia kwa dua, aipendayo na kisha hutoa Salam kwa kusema:*Asalamu aAla Nabiyyi wa Rahmat Allahi wa Barakatuhu,*

Asalamun aAlayna wa Ala Ibadi Illahi Salihina Salaam Aalaykum **kugeukia upande wake wa kulia na kisha anarudisha Uso upande wa mbele na kama mtu wa Kushoto yake atatoa Salam basi atamjibu.'***(Malik Muwwata)*

Naam..hio ni aina nyengine ya Tahiyyat kulingana na Mtizamo wa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kutoka katika Kitabu cha Hadith cha Muwwata Imam Malik.Na pia Hadith hii imenukuliwa na Imam Al Bayhaqi kutoka kwa Abu Ahmad Abd Allah Muhammad Ibn Hasan Al Adl kupitia kwa Abu Bakr Muhammad Ibn Jafar Al MuzakiKupitia kwa Muhammad Ibn Ibrahim kupitia kwa Ibn Bukayr kupitia kwa Imam Nafii na kumalizia kwa Imam Malik.

Na pia kuna hadith ya *Umm ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha* kutoka kwa Imam Malik isemayo kua:

عَنْ يَحْيَى بْنِ سَعِيدٍ الْأَنْصَارِيِّ عَنِ الْقَاسِمِ بْنِ مُحَمَّدٍ أَنَّهُ أَخْبَرَهُ أَنَّ عَائِشَةَ زَوْجَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَتْ تَقُولُ: إِذَا تَشَهَّدَتْ فِي الصلاة

التَّحِيَّاتُ الطَّيِّبَاتُ الصَّلَوَاتُ الزَّاكِيَاتُ لِلَّهِ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

Amesema Yahya Ibn Said Al Ansari kua amesema Al Qasim Ibn Muhammad kua Ummu ul Muuminin Aisha Radhi Allahu AnhaAlikua akisema katika wakati wa Kusoma Atahiyyat kua:Attahiyyat At Tayyibatu, As Salawatu, Az Zakiyyatu Lillahi, Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wahdahu la Sharika Lahu, Wa Ashhadu Anna Muhammadan aAabdu Allahi wa Rasuluhu, Asalamu Aalayka Ayyuha Nnabiyyu warahmat Allahi wabarakatuh.*(Muwwata Imam Malik)*

Naam..nadhani kwa mifano ya aina tu za Tashshhud, au Tahiyyat kulingana na vithibitisho vya Hadith basi itakua zimetutosheleza. Na Wanazuoni Wanakubaliana kua Tahiyyat zote zilizotajwa kwenye Hadith Sahih kua ni Tahiyyat zinazokubalika kusomwa ndani ya Sala kulingana na Mtu atakavyopenda mwenyewe katika Sala yake. Na inakubalika pia Kusoma Tahiyyat Moja katika Kikao cha kwanza na Tahiyyat nyengine katika kikaoCha Mwisho cha Tahiyyat.

Hivyo mbali ya kukubaliana kwao huko Wanazuoni juu ya kukubalika Visomo vyote vya Tahiyyat, lakini hata hivyo Wanazuoni wamekhitilafiana kuhusiana na Jawabu la Suali liulizalo kua: Ni Ipi Tahiyyat Bora zaidi

Kwani kwa Upande wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua:

Attahiyyat ya Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambayo ni ifuatayo:**Kama isemavyo Hadith yake kua:**

كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يُعَلِّمُنَا التَّشَهُّدَ كَمَا يُعَلِّمُنَا الْقُرْآنَ فَكَانَ يَقُولُ " التَّحِيَّاتُ الْمُبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ الطَّيِّبَاتُ لِلَّهِ سَلاَمٌ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ سَلاَمٌ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ "

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitufundisha Tahiyyat kama anavyotufundisha Qur'an na alikua akisema:**

At Tahiyyat, Al Mubarakatuh, As Salawatu Al Tayyibatu lillahi Salamu Alayka Ayyuha Nnabiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, Salamu Alayna wa Aala Aibadi Allahi Salihina, Ashhadu An Lai lah Illa AllahWa Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah*(Sahih Muslim, Sunnan Abu Daud, Sunan At Tirmidhii, Musnad Imam Ahmad)*

Na Ubora wake Tahiyyat hii ni kua Imetumia Neno *Al Mubarakat* ndani yake ambalo linaendana sambamba na maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo:

﴿فَاِذَا دَخَلْتُمْ بُيُوْتًا فَسَلِّمُوْا عَلٰٓى اَنْفُسِكُمْ تَحِيَّةً مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ مُبٰرَكَةً طَيِّبَةً ۗ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ﴾

Fa idhâ dakhaltum buyûtan fa sallimû ‘alâ anfusikum Taḥiyyatam min ‘indillâhi mubârakatan tayyibah, kadhâlika yubayyinullâhu lakumul-âyâti la‘allakum ta‘qilûn.*(Surat An Nur 24:61)*

Tafsir ***Hivyo Mnapoingia Majumbani Basi Amkianeni baina yenu Maamkizi Kutoka kwa Allah Yaliyojaa Baraka na Mazuri Sana Hivyo ndivyo pia anavyokubainishieni Allah juu yenu ili Mpate Kufahamu.***

Naam...kama tunavyoona kua hii pia ni Aya iliyobeba neno Tahiyyat yaani Maamkizi au Kuheshimu. Ambapo aya hii ndani*Allah Subhanah wa Ta'ala* anawafundisha Waja wake Tabia bora Na Adabu katika Majumba yetu.Kwa kuwaambia kua wanapokutana au wanapoingia Majumbani mwao Basi waamkiane kwa *Tahiyyat* kutoka kwa *Allah Subhanah wa Taala* ambayo ni *Mubarakan Tayyibatan* yenye Baraka na Yaliyo Bora ambayo ni *Salaam Alaykum wa Rahmat Allahi wa Barakatuh.*

Na hii ni kwa Sababu Kabla ya Kuja Uislam basi Waarabu walikua wanapokutana huamkiana kwa kuambiana *‘Hayyaka Allah!’* yaani ‘*Allah Akupe Uhai’* zaid hio ndio iliyokua *Tahiyyat* yao Waarabu. Lakini *Allah Subhanah wa Ta'ala* akawabadilishia Waislam Maamkizi hayo na kuwapatia Maamkizi bora zaidi yaani *Tahiyyatan Mubarakatan Tayyibatan* ambayo ni *Salaam Salatkum wa Rahmat Allahi wa Barakatuh.*

Na anasema *Mujaddid Ad Din AlHafidh* Imam Ibn Hajar Al Asqalani Al Shafii kua: ‘***Tahiyyat* ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ni sawasawa kimaana na *Tahiyyat* ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* isipokua ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ina neno *Al Mubarakatu* wakati ya Umar *Radhi Allahu Anhu* ina neno *Al Zakiyyatu.’***

Ambapo kama tulivyosema kua *Tahiyyat* ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ndio ya Madhhab ya Imam Al Shafii kwa sababu ina ukaribu zaidi na Aya ya 61 ya Surat An Nur iliyosema *Tahiyyat* bora kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala* ambayo ni *Mubaraka Tayyiban*, ambayo ni:

"التَّحِيَّاتُ الْمُبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ الطَّيِّبَاتُ لِلَّهِ سَلاَمٌ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ سَلاَمٌ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ"

At Tahiyyat, Al Mubarakatuh, As Salawatu Al Tayyibatu lillahi Salamu Alayka Ayyuha Nnabiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, Salamu Alayna wa Aala Aibadi Allahi Salihina, Ashhadu An Lai lah Illa Allah Wa Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah.

Na hio ni kwa upande mmojalakini tusisahau pia kua kwa upande mwengine wa pili pia hii ni kwa sababu Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii ni Fiqh yenye Msingi wa *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae ndie aliekua Mwanafiqh Mkuu wa Mji wa Makkah miongoni mwa Masahaba*Radhi Allahu Anhum* na Imam Al Shafii alianzia masomo yake katika Mji wa Makkah chini ya Mufti Mkuu wa Makkah Imam Muslim Ibn Khalid Zanj ambae alikua ni Muafrika mweusi, na Imam Sufyan Ibn Uyaynah na Imam Az Zuhri katika Mji huo wa Makkah baada ya kutoka katika maeneo ya Asqallani katika Mji wa Gaza nchini Palestina ambako ndiko alikozaliwa.

Naam...mji wa Gaza Palestina unaofisidiwa na Wazayuni sasa hivi kwa kufanya Muaji ya Kimbari ndani yake yanayopelekea kuuawa kwa Wapalestina zaidi ya 51,000, hadi wakati wa uandishi wa kitabu hiki miongoni mwao wakiwemo watoto zaidi ya 17,000 ndio Mji aliozaliwa Imam Muhammad Idris al Shafii.

Na kwa upande wa Tahiyyat ya Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik yenye neno *Az Zakiyyatu* basi ni *Tahiyyat* ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhum* na pia ndio ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*, ambao waliishi Madina ambayo ni:

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ ، الزَّاكِيَاتُ لِلَّهِ ، الطَّيِّبَاتُ الصَّلَوَاتُ لِلَّهِ ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ ، السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ . وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

Attahiyat lillahi, Az Zakiyyat Lillahi At Tayyibatu wa Salawatu lillahi Asalamu aAlayka Ayyuhan Nabiyyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuhu, Asalamun aAlayna wa Ala Ibadi Illahi Salihin wa Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammadan aAbduhu Wa Rasuluhu

Na tukiiangalia Fiqh ya Madhhab ya Imam Malik basi tunaona kua ni Fiqh inayoipa kipaumbele zaidi Mitizamo ya Masahaba*Radhi Allahu Anhum,* yaani vyanzo vya Fiqh kwao baada ya Qur'an na Hadith basi kinachofuatia ni Mitizamo ya Masahaba Wanazuoni *Radhi Allahu Anhum*walioishi Mjini Madina.

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na baadhi ya Wafuasi wa Imam Ahmad Ibn Hanbal (kwani Baadhi Wanafuata Tahiyyat ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*) basi wao wanafuata Tahiyyat ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kama tulivyosema hapo kabla, ambayo ni:

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

At Tahiyyatu Lillahi wa Salawatu wa Tayyibatu As Salamu Alayka Ayyuha Nabbiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, As Salamu Aalayna wa Aala Aibadi Allahi Salihina, Ashhadu An Lailaha Ila Allah wa Ashhadu Ana Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu

Na hii ni kwa sababu Mbali ya kua Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* alikua ndie Mwanafiqh wa Iraq miongoni mwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na hivyo kuziachia Fiqh za Madhhab ya ImamAbu Hanifa na Imam Ahmad Ibn Hanbal athari zake kimitizamo kutokana na kua Maimam wawili hawa walikua ni Maimam walioishi katika Ardhi ya Iraq katika Mji wa Baghdad na Mji wa Kufah.

Lakini pia tunapoiangalia hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* basi tunaona kua Ndio Hadith Sahih zaidi ya Tahiyyat inayokubalika na Maimam wote na ndio hadith pekee iliyonukuliwa na Maimamsita Wakuu wa Hadith na Kuthibitishwa Usahih wake kati ya Hadith zote za Tahiyyat.

Kama alivyosema Imam At Tirmidhii kua: '**Hadith hii ha Tahiyyat ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ndio Hadith Sahih zaidi miongoni mwa Hadith za Tahiyyat.'**

Na akasema pia Imam Al Bazzar kua: '**Kwa Mtizamo wangu basi Hadith Sahih zaidi ya *Tahiyyat* ni Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ambayo imenukuliwa na watu 20 tofauti.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi yeye anasema kua: **'Bila ya shakahakuna kutofautiana baina ya Wanazuoni kua Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua ndio Hadith Sahih zaidi, kama alivyosema Al Baghawi katika Sharh Sunnan yake, kua Ni Hadith iliyokubaliwa na wote na haina utofauti wa Maneno yake katika kunukuliwa kwake na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*ameinukuu kutokana na Mafundisho ya moja kwa moja kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

HUKMU ZA TASHAHUD/TAHIYYAT KATIKA SALA.

❖❖❖

Tunapoangalia kuhusiana na Hukmu za Tashahud/Tahiyyat basi tunaona kuaWanazuoni Wametofautiana kuhusiana na Hukmu za Tahiyyat Ndani ya Sala.Kwani kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua: '**Tahiyyat ya Mwanzo ya Sala hua ni Sunnah na Tahiyyat ya Mwisho ndio Moja kati ya Nguzo za Sala na hivyo hua Ni Wajib kusomwa.'**

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi wao wanasema kua: '**Tahiyyat Zote Mbili za Sala hua ni Sunna**, **Ila kuna Baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanaosema kua: Tahiyyat ya mwanzo hua ni Sunna na Tahiyyat ya Mwisho hua Wajib'**

Na tunapoangalia kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: '**Tahiyyat ya Mwanzo hua ni Lazima na Tahiyyat ya Mwisho hua ni Wajibu**. **Ambapo mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni wa Ilm ya Hadith.'**

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua kuhusiana na Tahiyyat kua: '**Kulingana na Mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab yetu basi ni kua Tahiyyat hua ni Wajib na ni Nguzo ya Sala**. **Na hivyo Mtu ni Lazima aisome, japo kwa kifupi tu hua inatosheleza na kuifanya Sala ya Mtu husika kutobatilika. Hivyo Mtu anaweza kuifupisha kwa kusema:**

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولاللَّهِ

Attahiyyatu Lillahi Salamu aAlayka Ayyuhan Nabiyyu wa Rahmat Allahi Wa Barakatuh, As Salamu aAlayna wa aAla Aibadi Allahi Salihiina Ashhadu an la ilaha Illa Allah wa Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah.'

Naam..yaani inakubalika kwa Mtu kusoma Tahiyyat bila kusema *Al Mubarakatu, At Tayyibatu, Zakkiyatu, As Salawatu,* na kufanya hivyo ndio kuifupisha kwake, lakini hua ni Vizuri zaidi kuisoma yote kwa urefu.Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Tahiyyat Fupi kabisa inayokubalika ni ile aliyoisema Imam Al Shafii na wengi Miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab yetu yaani kusema**:

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ السَّلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولاللَّهِ

Atahiyyat Lillahi Salaamun Alayka Ayyuha Nabiiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh Salamu Aalayna wa aAla Aibadi Allahi Salihiina Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah.

Na Imam Ibn Sura yj yeye amesema kua Tahiyyat Fupi inayokubalika ni:

التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ السَّلَامُ عَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولاللَّهِ

Attahiyyat lillahi Salaamun Alayka Ayyuha Nnabiyu, Salamun aAla Aibadi Allahi Salihiina Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu An Na Muhammad Rasul Allah*(Rawdha Talibin)*

Ama kuhusiana na Sala Fupi ya Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi hua ni *Allahuma Salli aAa Muhammad*. Hivyo kama Mtu akisema *Salallahu aAla Muhammad* basi juu ya kauli hii hua kuna mitizamo Miwili Juu yake. Kwani Muandishi wa Al Hawi (Al Qadhi Al Hafidh Al Imam Ali Ibn Muhammad Al Mawardi) Basi amesema kua kusema hivyo hua ni sawa na aina mbili za *Salam kwa kusema Salaam Alaykum, au Salaam Alaykum wa Rahmat Allahi wa Barakatuh* na kwani zote hua zinatosheleza.'

Ambapo kwa Upande wa Muandishi wa *Al Tadhhib Fi Fiqh Al Imam Al Shafii*(Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Fara Al Baghawi Al Shafii) basi amesema: '**Kama Mtu atasema Katika Tahiyyat yake *Allahuma Sali aAla Nabii* au atasema *Allahuma Sali aAla Ahmad* basi itamtosheleza**. **Kwani Imam Al Rafii amesema kua hata mtu akisema *Sala Allahu Aala Rasulihi* basi hutosheleza pia, na hata akisema *Salallahu Alayhi* hutosheleza pi**a*(Al Tadhhib.)*

Na amesema Shaykh ul Islami Al Alim Muḥammad Ibn Aḥmad Ibn Ḥamza Al Manūfī Al Miṣrī Al Anṣārī Shams Al DīnAl Ramli Al Shafii kua: '**Ukweli ni kua hata kama mtu katika Kushuhudia**

kwake katika Tashshahud ya Sala atasema *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah Wa Anna Muhammadan Rasuuluhu* basi itatosheleza pia, kwani sikuwahi kuona mimi aliesema kua neno *Aabduhu* ni sehemu ya Lazima katika kushuhudia'*(Hashyat Al Ramli aAla Asna Matalib)***

Na katika Kufafanua kwao Wanazuoni kuhusiana na Maneno Muhimu yaliyomo kwenye Tahiyyat ambayo yanapelekea kuifanya hata Attahiyat fupi ikubalike au Salat An Nabii fupi ikubalike na kutokua ni yenye kubatilisha kua:

Ama kuhusiana na Tahiyyat basi ni wingi Tahiyya ambao humaanisha Heshima na kuna wanaosema ni Ufalme, na kuna wanaosema ni Ukubwa na kuna wanaosema kuaNi Uhai.

Na Tahiyyat imekua katika hali ya wingi kwa sababu Wafalme huamkiwa, huheshimiwa katika hali ya Wingi, na hivyo Tahiyyat humaanisha kua Heshima zote au Maamkizi Matukufu yote yanastahiki kwake yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo kwa upande wa ImamAl Khattabi na Imam Al Baaghawi basi wao wanasema kua: **'Hakuna kitu chochote katika Salam za Ibn Adam ambazo ni zenye kufaa na kustahiki kwa ajili ya Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* , kwani maneno ya Ibn Adam hayawezi kuelezea sifa stahiki za Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na ndio maana ikaambiwa: Semini Attahiyyat yaani aina za kumssif na kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* .'**

Ambapo kwa upande wa Imam At Tabari basi anasema kua: **'Inawezekana ikawa neno Tahiyyat linamaanisha maana nyengine zilizoelezewa hapo kabla na hivyo maana yake ya Salam hua ni yenye kufaa zaidi katika sehemu hii.'**

Na kuhusiana na Zakiyyat na Tayyibat katika Hadith ya Umar Ibm Al *Khattab Radhi Allahu Anhu* humaanisha Uongezekaji wa Vitu na mambo Masafi yaliyo bora, na kuna Wanaosema kua ni Sala, na wanaosema ni Dua na pia. Yaani hivi vyote ni Vyenye kustahiki kwake yeye *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwa upande wa Imam At Tabari basi anasema kua: **'Tayyibat humaanisha Matendo ya Amali njema ambazo malio yake kwa anaeyafanya hua ni kwa ajili ya Akhera tu. Yaani hii ni kuhusiana na Maneno Mazuri ikiwemo maneno ya kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Dhikr Allah. Na kuna wanaosema kua ni Kauli njema kama Dua na Dhikr na kua wanaosema kua ni Amali njema kwa ujumla ikiwemo Sala za Fardhi na za Sunna ambazo bila yautekelezwaji wake basi hua haiwezekani kumtukuza kistahiki kwa Sifa zake. Hivyo Tayyibat hua ni Amali njema na Sala na kila maamrisho ya Sharia au matendo yote ya Ibada au Dua au pia Rehma za *Allah Subhana wa Ta'ala* kwa Waja wake. Na imesemwa kua Tahiyyat ni vvitendo vya Kauli za Ibada na mambo mema kama Sadaka na Zakka na Sala na Ibada nyenginezo.'**

Ambapo kwa upande wa Hadith ya Abd Allah Ibm Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema *Al Mubarakatu, Al Salawatu* kumaanisha Baraka na Sala na mambo mema yote. Kama ilivyo kwenye hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* amesema ila kwake yeye basi herufi Waw imefutwa kwa ajili ya Kufupisha, na hii hua inakubalika katika Lugha zote.

Na hivyo maana ya Hadith ni kuaTahiyyat yaani Maamkizi na kila kinachofuatia baada yake*(Mubarakat, Tahiyybat, Zakiyyat, Salawat)* hua ni Lillahi yaani ni vyenye kua ni kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu peke yake na si kwa Mwengine yeyote.

Ambapo kuhusiana na *Asalam Alayka Ayyuha Nabbiy wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, Asalamu aAalayna wa Aala Aibadi Alahi Salihiina*

Basi hua ni kuomba Hifadhi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Ulinzi wake,na Kumtukuza kwake *Allah Subhanah wa Taala*Kwani Salam ni Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala,* na Makadirio yote ni kutoka kwake, na Hifadhi juu ya kila kitu ni kutoka kwake kwani yeye ndie Msimamizi wa uhakika juu ya kila Mtu.

Kama inavyosemwa *Allah Maak* maneno ambayo humaanisha kua *Allah Subhanah wa Taala* yuko pamoja nawe Kiulinzi, Kiusaidizi, Kihuruma na Kimapenzi. Yaani hua ni Kumaanisha kua uko katika Uokovu na Usalama kutokana na Usimamizi wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu yako. Na hii huweza kua ndio chanzo cha Mafanikio na Furaha ya Milele juu yako, kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema*Salamun aAla as-habi Al Yamini* - Salam iwe juu ya watu wa Kulia.

Na faham kua kuhusiana na *Al Salam Alayka Ayyuha Nnabiyu, Al Salam Alayna na Al Salaam aAla Aibadi Allahi Salihiina* basi hua inakubalika kuziondoa Heruf Alif na Lam na hivyo kusemwa *Salam Alayka Ayyuha Nabbiy, Salamu Alayna Salamu aAla Aibadi Allahi Salihiina*. Haya yote yanakubalika na hakuna kutofautiana juu yake, ila kutumia Alif na Lam hua ni bora zaidi, na kuna Hadith za Tahiyyat Katika Sahih Bukhari na Muslim ambazo hazikutumia Alif na Lam.

Hio ni katika Tahiyyat ya Mwanzo tu, kwani kuhusiana na Tahiyyat ya Mwisho wa Sala basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wametofautiana juu yake kuhusiana na hili la Alif na Lam.

Kwani kuna wanaosema kua inaruhusika kutumia njia zote mbili kote koteKwenye Tahiyyat ya kwanza na ya Pili. Na kuna wanaosema kua kutamka Alif na Lam hua ni Bora zaidi, na kuna wanaosema Kutumia Alif na Lam ni Lazima.

Na anasema Shaykh ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: **'Inaruhusika kuiondoa kuitaamka herufi Alif na Lam na pia kuiondoa na hii inathibitishwa na mifano iliyoo kwenye Hadith Sahih za vitabu vya Sahitayn.'**

Na Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani anasema kua: 'Haikutokea katika Sanad yeyote ya Hadith za Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahuu Anhu* kutokua na herfu Alif na Lam ila kua kutokukubaliana katika hadith ya Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* na hii ni kutokana na upekee wa wanukuaji wa Hadith hio'

Ama kuhusiana na *Aala Aibadi Allahi Salihiina* basi Imam Al Zajjaj anasema kua: Kuna Wanazuoni waliosema kua *Aibadi Allahi Salihiina* hua ni wale wenye Kutekeleza Majukumu yao kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu na Hapo hapo wakatekeleza Majukumu yao juu ya Waja wenzao.

Ama kuhusiana na Kuwatumia Salam basi Rehma na Baraka za Allah huwafikia Waja hao,na ukitumia herufi Alif na Lam basi ndani yake huwajumuisha na viumbe Majini wema pia kwa ujumla.

Ama kuhusiana na maneno ya Shahada yaani *Wa Ashhadu Anna Muhammadan Aabduhu wa Rasuluhu* basi Wanazuoni wa Lugha wanasema kua: 'Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* niIbn Adam ambae ni mwenye kustahiki kusifiwa kutokana na jua na Sifa nyingi zilizo

bora.Ambapo amesema Imam Ibn Faris kua: 'Na hii ndio Sababu inayompelekea Mtume wetu *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* kupewa Jina la Muhammad.''

Yaani kutokana na Kua na Sifa nyingi zilizo bora basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* amewajaalia Wazazi wake kumpa jina hili la Muhammad.

Ama kuhusiana na maneno *Allahuma Sali wa Salim aAla Muhammad,* hua yanamaninisha kuashiria mwisho wa Sala na hivyo Kuhitajika kwa Kisomo cha Dua kinachofuatia kabla ya kutolewa Salam ya Sala. Na hivyo humaanisha kua Inaruhusika kuomba Dua yeyote Mtu aitakayo kuhusiana na Mambo ya Kiakhera na Kidunia yasiyokua ya Dhambi.Huo ndio Mtizamo wa Madhhab yetu ya Imam Al Shafii na ndio Mtizamo wa Wengi miongoni mwa Wanazuoni.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao Wanasema kua haikubaliki kuomba Dua yeyote isipokua zile zilizomo ndani ya Qur'an na Hadith.Na hivyo kutokana na hali hii basi wengi Miongoni mwa Wanazuoni, wana mtizamo wa kua Katika Tahiyyat ya Mwisho hua si Wajibu kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ila kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: 'Ni Wajibu kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya Shahada ya Tahiyyat ya Mwisho hivyo yeyote yule atakaewacha kumsalia *Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* baada ya Kuhushudia ndani ya Tahiyyat ya Mwisho basi Sala yake hua ni Batili
Na ingawa Kuna Hadith si katika Sahih Muslim.Inayothibitisha kua ukifanya hivyo basi Sala yako hua imekamilika, lakini hadith hio si sahih kwani ina maneno yaliyoongezwa juu yake.'

Kwani hapa imesemwa hivyo kwa sababu ya kua kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: '**Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Kikao cha Mwisho cha Tahiyyat hua hakuna Ulazima, ila ni Sunna inayotiliwa Mkazo'***(Imam Shurunbulali katika Nur Al Idah)*

Na akasema tena Imam Abu Ikhlas Hasan Ibn Ali Ibn Shurunbulali Al Wafai Al Hanafi katika Maraqi Al Falah kua: **'Kujizoesha bila kukosa Kumsalia *Rasul Allah Aalallahu Alayhi wa Salam katika* katika Tahiyyat ya mwisho bila dharura hua ni kosa.'***(Maraqi Al Falah)*

Na anasema Shaykh Ul Islami Burhan Ad Din Abu Hasan Ali Ibn Abdul Jalil Abu Bakr Ibn Khalil Abu Bakr Habib Al Marghinani Al Rashdani Al Hanafi kua: **'Ama kuhusiana na Hadith zenye kuzungumzia kuhusiana na kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya Shahada ya Tahiyyat ya pili, basi ni hadith ambazo hazina nguvuna hivyo mtu atakaewacha hua hajafanya kosa, ila ni Sunna kufanya hivyo.'**

Na pia kuna kauli moja kutoka kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal ambayo amenukuliwa akisema kua: **'Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya Shahada ya Tahiyyat ya mwisho hua ni Sunna na si Wajibu na wala si Nguzo ya Sala, hivyo kama mtu akiwa hakufanya hivyo kwa makusudi basi Sala yake haijabatilika, na hii ni kwa sababu Hadith zinazonukuliwa kuthibitisha Wajibu wa kufanya hivyo na wanaosema kua ni Nguzo ya Sala, basi Hadith hizo hazikuweka wazi juu yake jambo hilo, hivyo kikanuni basi hua hakuna ulazima.'***(Sharh Al Mumti)*

Imam Abu Tayyibi Al Tabari aliulizwa: **'Hivi Kwanini katika Wakati wa Kusoma Tahiyyat na**

Kumsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hua inatumika hali ya Mtu wa pili badala ya hali ya Mtu wa Tatu?'

Yaani badala ya Kusema*Asalaamu Aala Nabiiy* - Salaam zimfikie Nabii inasemwa *Asalaam Alayka Ayyuha Nabii Salam* Zikufikie Juu yako Ewe Nabii?

Imam Abu Tayyib akajibu: 'Hii ni kwa sababu sisi Waislam hua tunafuata Maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kupitia katika yale aliyowafundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum.*

Yaani hii hua ni sawa na pale Mtu mwenye kufanya anapokua Ibada anappkua anafungua Mlango wa Ufalme kwa Salam, na hivyo hua ni wenye kuingia kwenye Maeneo Matukufu ya yule Aliehai na Asiekufa.

Hivyo Macho yao hua ni yenye kupata utulivu kutokana na Maombi yao, kudhihirishiwa kua ni yenye kukubalika kupitia kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae ni Mwingi wa Huruma, Rehma na mwenye kuambatana na Baraka zinazowanufaisha wale wanaomfuata.

Hivyo watu hao walipoingia kwenye Sehemu hio Tukufu basi wakamuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam Habib Allah* akiwa ndani ya eneo Tukufu la anaependwa nae yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Hivyo watu hao wakawa ni wenye kumsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema *Asalaam Alayka Ayyuha Nabiyyi Salallahu Alayhi wa Salam.'*

Ambapo kwa Upande wa *Mujaddid Ad Din Al Hafidh* Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi yeye anasema kuhusiana na Jawabu la suali hilo hilo kua: 'Kuna utofauti baina ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusema hivyo katika wakati alipokua hai, kua alisema *Asalaam Alayka Ayyuha Nabbiyu* Kwa kutumia hali ya Mtu wa Tatu, na baada ya Kufariki kwake.Lakini imethibitishwa katika Ilm kua imesema *Asalaam Alayka Ayyuha Nabiyyu* hata pale baada ya kufariki kwake na hii ni kulingana na namna yalivyokua maamrisho yake na mafundisho yake.'

Imam Ibn Hajar Al Asqallani anaendelea kusema kua: **'Kama suali litakua ni kwanini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamrisha isemwe *Ayyuha Nabii* na isisemwe *Ayyuha Rasul* wakati Rasul ni Jina linalojumuisha yote? Na ndio linaloainisha Jukumu lake la Utume kwa Watu wote? Hivyo Jibu la suali hili ni kua, Hikma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifanya hivyo kwa sababu ya kutaka Kuyatumia na kuyajumuisha Majina yote mawili Sambamba.'**

Na hii ni kwa sababu Utajo wa mwanzo ni mwanzoni mwa Tahiyyat kwa Jina la Nabii -*Asalaam Alayka Ayyuha Nabiiyu*. Lakini baada ya hapo katika kushuhudia ndaninya Tahiyyat basi Shahada imetumia utajo wa pili wa *Rasul Allah* mwishoni mwake kwa kusema *Wa Ashhadu Anna Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu'.*

Na pia kuna wanaosema kua Hikma ya kutumika neno Nabii ni katika Kuelezea Unabii wake Katika mfano wa Aya za Mwanzo ziliposhuka aliposhushiwa Wahy kwani kwanza ilianza:

﴿ٱقۡرَأۡ بِٱسۡمِ رَبِّكَ ٱلَّذِي خَلَقَ﴾

Iqraa Biismi Rabbika ladhii Khalaqa - *Soma Kwa Jina la Mola wako ambae ndie alieumba kila kitu**(Surat Al Alaq 96:1)*

Na kisha ndio ikafuatia:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡمُدَّثِّرُ ۝ قُمۡ فَأَنذِرۡ﴾

Ya Ayyuha Al Mudathir-*Ewe Uliejifunika Gubigubi.*

Qum Faandhir - *Amka Uonye!**(Surat Al Mudathir 74:1-2)***

Kisha Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani anaendelea kusema kua; '**Naimetajwa katika Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na utofauti wa wakati wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* hivyo imesemwa katika wakati alipokua hai na pia imesemwa baada ya kutokuwepo kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Kama katika Hadith ya Imam Bukhari ambayo ameinukuu katika hali ya kuomba Ruhusa kutoka kwa Abu Muammar kupitia kwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* baada ya kuinukuu Hadith ya Shahada ambapo ndani yake amesema kua:**

Alipokua pamoja nasi basi tulisema *Asalaam Alayka Ayyuha Nabiyyu,* na alipofariki basi tukawa tunasema *Asalaam Aala Nabiyy.*

Imam Ibn Hajar Al Asqallahi anaendelea kusema kua: '**Abu Awana, Al Siraj, Al Jawzaqi, Abu Nuaym Al Isfahani na Al Bayhaqi wote wamemukuu Hadith hii kutoka katika Sanad Tofauti**, **Ambapo katika Hadith ya Abu Nuaym ambae ni Mwalimu wa Imam Al Bukhari basi tunaona kua inasema:**

قال ابن مسعود وهنا الفائدة قلنا (السلام عليك أيها النبي والنبي بين ظهرانينا) أي وهو حي يعيش بين ظهراني أصحابه قال ابن مسعود (فلما مات عليه الصلاة والسلام قلنا السلام على النبي)

Amesema Ibn Masud*Radhi Allahu Anhu*, : 'Na hii nakupeni faida, sisi tulikua tukisema Asalaam Alayka Ayyuha Nabiyyu, wakati Nabii *Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua pamoja nasi miongoni mwetu' Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*akasema tena kua: 'Hivyo alipofariki *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tukawa tunasema *Salaamun Aala Nabbiy'*

Na kwa upande mwengine basi anasema Imam Ibn Abd Razzaq kua:'Ametuambia sisi Ibn Jurayj kua ametuambia sisi Ata'a kua Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua wakisema wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa hai kua: *Asalaama Alayka Ayyuha Nabiiyu, Na alipofariki wakawa wanasema Asalaam aAla Nabiiyi.'*

Na hii ni Hadith Sahih, na pia amesema Said Ibn Mansur kua amesema Abu Ubaydah Ibn Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Ameniambia Baba yangu (Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*) mimi kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiwafundisha Tashahud na akaisoma.'**

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema Sisi tulikua *tukisema Asalaamun Alayka Ayyuha Nabbiyu* wakati alipokua hai. Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Hivyo ndivyo tulivyofundishwa sisi, na hivyo ndivyo tunavyojua.''

Kwa maana hio basi ingawa kuna mitizamo tofauti kulingana na Hadith husika lakini hata hivyo ni bora katika Tahiyyat/Tashahud zote mbili ya kwanza na ya mwisho kusema:*Asalaam Alayka Ayyuha Nabiiyu*, Kwani hivyo ndivyo ilivyokuja kwenye Hadith sahih.

Ama kwa upande mwengine basi katika Kisomo cha Tahiyyat kuna suali pia la Kujiuliza ambalo ni kua: '**Kwanini baada ya Kumsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi,* basi hua tunajiombea sisi wenyewe na kisha ndio Tunawaombe Waja wema *wa Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema:*Asalamun Alayka Ayyuha Nabiiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh asalamu Alayna wa aala Aibadi Allahi Salihiina.'***

Naam anasema Al Qadhi Al Imam Nasir Ad Din Al Baydawi Al Shafii kua: '***Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* amewafundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* katika Tahiyyat kutofautisha katika kumtumia Salam yeye mwenyewe kwanza na hii ni Kutokana na Darja yake na Heshima na haki aliyokua nayo juu ya watu wa Umma wake.Kisha akawaamrisha Masahaba zake hao *Radhi Allahu anhum* kujitumia Salam wao wenyewe, kwanza na hii ni katika kuonesha namna wanavyotakiwa. Kujijali kwani hilo ndio Jambo Muhimu zaidi kwa Ummah wa Kiislam Na kisha akawaamrisha Kuwatumia Salam Waja wema, na hivyo kuwaonesha Umuhimu wa Kuwaombea Waja wema ambao ni miongoni mwa Waislam wenzao.'**

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi yeye anasema kua: '**Huu ni Uthibitisho wa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhiwa Salam* anatufundisha kua Tunapotaka kuomba Dua basi kwanza tunakiwa Kujiombea Nafsi zetu**. **Kama ilivyosemwa katika Hadith ya Ubbay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* kua: Kila mara *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua anataka kumuombea Mtu Dua basi hujianzia na yeye mwenyewe kwanza.'***(Imam Al Tirmidhi)***

Kama ilivyooneshwa ndani ya Qur'an pale Nabii Nuh Alipoomba Dua kwa kusema:

﴿ رَّبِّ ٱغۡفِرۡ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَن دَخَلَ بَيۡتِيَ مُؤۡمِناً وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَاتِ وَلاَ تَزِدِ ٱلظَّالِمِينَ إِلاَّ تَبَاراً﴾

Rabbi ighfir lee waliw<u>a</u>lidayya waliman dakhala baytiya mu/minan walilmu/mineena waalmu/min<u>a</u>ti wal<u>a</u> tazidi al*<u>dhdha</u>*limeena ill<u>a</u> tab<u>a</u>ran*(Surat Nuh 71:28)*

*Tafsir:**Ewe Mola wangu Nisamehe mimi na Wazee wanguNa Kila Atakaeingia Ndani ya Nyumba yangu Akiwa Muumini Na Waumini wa Kiume na Waumini wa Kike na Usiwazidishie Madhalimu isipokua Maangamizo.***

Na pia kama Alivyoomba Nabii Ibrahim kwa kusema:

﴿رَبِّ ٱجۡعَلۡنِي مُقِيمَ ٱلصَّلاَةِ وَمِن ذُرِّيَتِي رَبَّنَا وَتَقَبَّلۡ دُعَآءِ ۞ رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ يَوۡمَ يَقُومُ ٱلۡحِسَابُ﴾

Rabbi ijAAalnee muqeema al<u>ss</u>al<u>a</u>ti wamin <u>dh</u>urriyyatee rabban<u>a</u> wtaqabbal duAA<u>a</u>/-I; Rabban<u>a</u> ighfir lee waliw<u>a</u>lidayya walilmu/mineena yawma yaqoomu al<u>h</u>is<u>a</u>bu*(Surat Ibrahim 14:40-41)*

Tafsir: Ewe Mola wangu Nijaalie kua ni mwenye Kusimamisha SalaNa Kizazi change - Ewe Mola Wangu Nikubalie Dua Yangu Mola Wangu Nisamehe Mimi na ***Wazee wangu na Waumini katika Siku Ambayo Itasimamishwa Hesabu na kuhesabiwa.***

Ambapo hadithi hio ya Imam At Tirmidhii ni ile ambayo ndani yake amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* amesema Ubbay Ibn Ka'ab *Radhi Allahu Anhu* kua:

عن ابن عباس رضي الله عنهما عن أبي بن كعب: أن رسول الله صلى الله عليه وسلم كان إذا ذكر أحدا فدعا له بدأ بنفسه . قال أبو عيسى : هذا حديث حسن غريب صحيح

Alikua Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam **alikua kila anapotaka kumuombea Dua mtu yeyote yule basi huanza kwa kujitaja yeye kwanza**.' Ambapo amesema Abu Isa Al Tirmidhi kuhusiana na hadithi hii kua: '**Hii ni Hadith ambayo ni Hasan Sahih na ina upekee'**

Na kwa upande wa Imam Muslim basi pia amesema kua: '***Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam*** **alikua kila anapotaka kumtaja Nabii yeyote yule basi huanza kwa kujitaja yeye kwanza**.'

Ambapo amesema Imam Al Fakhani kua: '**Mtu mwenye Kuomba Dua basi anatakiwa Awombee Mitume, Malaika na Waumini ili Maneno yake ya Dua hio yawe ni yenye kuendana sambamba na Nia yake.'**

Na amesema Imam Al Hakim Al Tirmidhi kua:**'Yeyote anaetaka kunufaika na Dua za Kuombewa na Waumini katika Tahhiyat za Sala zao basi na ajitahid awe *min Aibadin Salihiina* yaani Miongoni mwa Waja wema.'**

Kwani kwa upande mwengine basi kuna hadith pia zinazothibitisha kua *RasulAllah Salallahu Alayhiwa Salam* alikua akifanya hivyo pale alipokua anataka kuwaombea Dua Mitume wengine.Na kuna Hadith zinazothibitisha kua ilikua si lazima kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Pale anapotaka kumuombea Dua Mtu wa Kawaida kua Ajitaje yeye.

Kwa Mfano katika kisa cha Kusilimu kwa Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* pale aliposilimu basi alimuomba *Rasul AllahSalalahu Alayhi* wa *Salam* kua amuombee Msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na kua aliwaua Waislam wengi katika wakati wa Ukafiri wake.

Lakini hata hivyo *RasulAllah Salallahu Alayhiwa Salam* akamwambia Khakid Ibn *Walid Radhi Alahu Anhu* kua: 'Mtu anaposilimu bas Hua ni swa na aliezaiwa upya kwani Dhambi zake zote alizofanya alipokua Ukafiri hufutika.'

Lakini Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhuakamsisitizia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* maru tatu hadi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuombea Msamaha Khaklid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,*bila ya kujitaja yeye mwenyewe.

Mfano mwengine ni wa Kisa cha Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alipokua Mdogo, ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuamrisha kua Asali pamoja nae pembeni yake.Lakini hata hivyo Mtoto Abd Allah Ibn Abbas hakusali pamoja nae, *na Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* alipomaliza kusali na kumuuliza Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema: 'Kwanini nilipokuamrisha Usali pamoja nami pembeni yangu hukusali.'

Ambapo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Ya *Rasul Allah* hakika wewe Darja yako ni kubwa sana mbele yangu mimi kiasi ya kua Haiwezekani kua Mimi na wewe Tusimame pamoja bega kwa bega mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'

Hapo *Rasul Allah SalallahuAlayhi wa Salam* akatabasam na kisha akasema: 'Ewe Mola wangu Muongezee Mtoto huyu Ufahamu wa Ilm ya Dini.'

Naam na Dua hio ikakubaliwa hivyo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alipokua mkubwa akawa ni Bahari ya Ilmu.

Naam, tunapoangalia kwa upande mwengine katika Shahada ndani ya Tashahud au ndani ya Tahiyyat ambayo ni maneno yasemayo:**Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammadan Aabduhu wa Rasuluhu.**

Basi katika hadith yenye Attahiyyat ya *Ummu ul Muuminina* Aisha *Radhi Allahu Anha*tunaona kua ndani yake imebeba Shahada isemayo*: '**Attahiyyat At Tayyibatu, As Salawatu, Az Zakiyyatu Lillahi, Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wahdahu la Sharika Lahu, Wa Ashhadu Anna Muhammadan aAabdu Allahi wa Rasuluhu, Asalamu Aalayka Ayyuha Nnabiyyu warahmat Allahi wabarakatuh.'***(Muwwata Imam Malik)*

Ambapo katika kumshuhudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi ametumia maneno *Wahdahu la Sharika lahu.*Ambapo maneno haya pia yanaonekana katika Hadith ya Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* iliyomo katikaSahih Muslim na pia katika Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* iliyonukuliwa na Imam Ibn Abi Shaybah.

Na katika hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* iliyonukuliwa na Imam Ad Daraqutni.Ambapo hata hivyo Wanazuoni wanasema kua Sanad zake hadith hii ni dhaifu.Na hivyo hadith iliyosahih kuhusiana na Shahada ya kumshuhudia *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Tahiyyat ni Hadith ya Umar Ibn Al Khattabu *Radhi Allahu Anhu* na Hadith Ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ambazo ndani yake zimebeba maneno ya Shahada isemayo: *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah*,tu!

Na Wanazuoni wanasema kua maneno *Wahdahu la Sharika lahu* ni yaliyongezwa na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* na mwenyewe Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* amesema kua **: 'Mimi nimeongeza maneno *Wahdahu la Sharika Lahu.'***

Ambapo kuhusiana na Shahada ya kumshuhudia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* basi pia kuna Hadith zilizotumia maneno: '***Ashhadu An La Ilaha Illa Allah Wa Ashhadu Anna Muhammadan aAabdu Allahi wa Rasuluhu.'***

Na kuna zilizotumia Shahada ya : *'**Ashhadu An La Ilaha Illa Allah, Wa Ashhadu Anna Muhammadan Rasul Allah*** kama Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* katika Sahih Muslim.

Na pia kuna hadith ambazo zimetumia Shahada ya: *'**Ashhadu An La Ilaha Illa Allah, Wa Anna Muhammadan Rasul Allah.'***

Yaani hazikutumia neno*Wa Ashhadu* -Na Nnashuhudia katika upande wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,*kwa sababu zimejumuisha Shahada moja kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam.*Ambapo hata hivyo zote ni shahada zinazokubalika kihukmu na kisharia.

Kwani kisichokubalika ni kubadilisha maneno kuweka mbele nyuma kama inavyoonesha Hadith ifuatayo:**'Anasema Imam Abd Al Razzaq kua amesema Ibn Jurayj kua amesema Ataa ambae amesema kua:Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akiwafundisha Watu Shahada, basi kuna Mtu mmoja alisema: '*Ashhadu An La Ilaha Illa Allah Wa Ashhadu Anna Muhammadan Rasul Allah wa aAabdu Allah*Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam***

akasema: La hakika Mimi kwanza nilikua Mja kabla ya Kua *Rasul Allah* hivyo sema: '*Ashhadu An La Ilaha Illa Allah, Wa Ashhadu Anna Muhammadan aAabduhu wa Rasuluhu.'*

Hivyo hilo ni moja kati ya masharti ya Tahiyyat ambapo mengineyo ni yafuatayo;

1-Msomaji Tahiyyat anatakiwa awe ni mwenye Kusoma kimya Kimya bila kusikika na watu wengine lakini hapo hapo akiwa ni mwenye Kujisikia yeye Mwenyewe katika kusoma kwake.

2-Msomaji awe ni mwenye kusoma Tahiyyat hila ya Kukatisha, hivyo kama akikatisha basi Tahiyyat hio hua haihesabiki.

3-Msomaji Tahiyyat anatakiwa asome huku akiwa amekaa Kitako, isipokua pale inapokua ana Udhuru unaokubalika Kisharia kua haiwezekani kwake kukaa Kitako.

4-Msomaji wa Tahiyyat anatakiwa aisome Attahiyyat kwa Lugha ya Kiarabu.

5-Msomaji wa Tahiyyat anatakiwa awe na umakini katika usomaji wake ii asibadilishe maneno, wala asibadilishe mfumo kwa neno la mbele kuweka nyuma n.k.

KUNYOOSHA KIDOLE KATIKA TASHAHUD/TAHIYYAT YA SALA.

❖❖❖

Kunyoosha Kidole katika wakati wa kushuhudia ndani ya kisomo cha Tahiyyat au Tashhud hua pia ni miongoni mwa Masharti yake, na ni Sunna ya *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*kama inavyosema Hadith ifuatayo ambayo inasema: '**Anasema Imam Malik kua amesema Muslim Ibn Abi Maryam kua amesema Ali Ibn Abd Rahman Al Muawi kua:**

رآني ابنُ عمرَ وأنا أعبثُ بالحصَى في الصَّلاةِ ، فلمَّا انصرفَ نَهاني وقالَ اصنَع كما كانَ رسولُ اللَّهِ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ يصنعُ قلتُ وكَيفَ كانَ يصنعُ ؟ قالَ : كانَ إذا جلسَ في الصَّلاةِ وضعَ كفَّهُ اليُمنَى علَى فَخِذِهِ ، وقبضَ يعني أصابعَهُ كلَّها وأشارَ بإصبعِهِ الَّتي تلي الإبهامَ ، ووضعَ كفَّهُ اليُسرَى علَى فَخِذِهِ اليُسرَى

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* aliniona mimi wakati nikiwa nnasali huku nikigusagusa changarawe (zilizo pembeni yangu).Hivyo baada ya kumaliza Kusali, basi Abd Allah Ibn Umar akanifuata na Kunikataza huku akisema: 'Unaposali basi fanya kama alivyokua akifanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hivyo nami nikamuuliza: 'Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali vipi?.'

Ambapo Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Alikua anapokaa katika Tahiyyat basi huuweka mkono wake wa Kulia Juu ya Paja la Kulia, na akiwa ameufunga Ngumi Mkono kwa vidole vyake vyote, huku akiwa amenyoosha kidole chake cha Shahada kilicho karibu na Kidole gumba, Na alikua akiuweka mkono wake wa kushoto juu ya Paja lake la kushoto, Hivyo

ndivyo alivyokua akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*'*(Muwaata Imam Malik, Sahih Muslim)*

Hivyo hii ni moja kati ya Hadith zinazoeleszea kuhusiana na Kunyoosha Kidole cha Shahada katika Shahada ya Kisomo cha Tahiyyat, ambapo Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Hikma ya Kitendo hiki cha Kunyoosha kidole cha Shahada kwani kuna wanaosema kua Hua ni Ishara ya Tawhid yaani kuashiria kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Mmoja tu na ndie pekee anaestahiki kuabudiwa kwa Haki.

Na kuna wenye Mtizamo wa kama anavyosema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua: '**Amesema Muslim Ibm Abi Maryam kua, Kunyoosha kidole katika Tahiyyat hua kunaashiria kama silaha ya Upanga dhidi ya Shaytan na hivyo unaponyoosha kidole cha shahada basi hua husahau kitu ndani ya Sala yako.'**

Na pia kuna wenye Mtizamo wa Imam Al Baji ambae amesema kua: **'Kunyoosha Kidole katika Shahada ya Tahiyyat hua ni kwenye kumpelekea Mtu anaesali kuukimbiza usahaulivu na kua ni mwenye kumbana Shaytan na Minong'onezo yake.'**

Kwani Hadith inatuonesha kua Kidole cha Shahada katika wakati wa Tahiyyat hua ni chenye kuelekezwa Kibla.

Na amesema Shihab Al Din Al Ramli, Fath Al Rahman bi Sharh Zabad Ibn Raslan, kua: **'Kimeitwa kidole cha shahada. Kwa sababu inatajwa wakati wa ugomvi na matusi, na pia kinaitwa: Tasbih. Kwa sababu inahusu tauhidi na kuinuliwa; Kwa sababu sifa ni kutukuka.'**

Na Al Khatib Al Shirbini, Mughni Al Muhtaj Al Muhtaj I'l-Minhaj kua : **'(Na huitwa Tasbih) kwa rai zote mbili, na imeitwa kwa kasra ya "ba" inayofuata kidole gumba. Kwa sababu inahusu imani ya Mungu mmoja na utakaso, na pia kinaitwa kidole cha shahada. Kwa sababu inarejelewa wakati wa kugombana na kuapa.'**

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi anasema kua: '**Kunyoosha Kidole cha Shahada katika Upande wa Kibla katika wakati wa kisomo cha Tahiyyat hua kunaashiria Nia ya kuthibitisha Kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Kua na Ikhlasi katika kuashiria hivyo, wa *Allahu wa Rasuluhu Aalam.'***

Ambapo kwa upande wa Imam Sulayman Ibn Muhammad Al Bujarimi Al Shafii basi anatufahamisha zaidi kwa kusema kua: '**Hua ni Makruh kunyoosha Kidole cha Mkono wa Kushoto, hata kama ikiwa Mtu husika amekatika Kidole cha Shahada cha Mkono wa Kulia, hivyo umuhimu wa Sunna ya kunyoosha kidole kwa Mtu asiekua na kidole cha Shahada cha mkono wa kulia hua haupo kwa yule asiekua na Kidole cha Shahada cha mkono wa Kulia.**

Na haitakiwi Kunyoosha Kidole cha Mkono wa Kushoto kwa sababu Sunnah ya Vidole vyote vya mkono wa Kushoto hua ni kuvinyoosha. **Kwa maana hio basi Hata kama Mtu atakua hana kidole cha Shahada cha mkono wa Kulia basi hairuhusiki kwake kunyoosha kidole chengine chochote kile, kwa sababu Kidole cha Shahada hua hakina mbadala wake.**

Na kwa upande wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii basi Kunyoosha Kidole cha Shahada cha mkono wa Kulia hua ni Sunnah iliyotiliwa mkazo, hivyo Mtu anaesali Hutakiwa Kunyoosha Kidole hicho pale katika Wakati wa Kukanusha kua Hakuna Mola Isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* yaani katika Maneno *Illa Allah,* kwani hayo ndio maneno yanayokana Shirk ya kumshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kuabudu,na hivyo kuashiria Tawhid yaani Kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani amesema pia Abd Allah Ibn Zubayr Radhi Allahu Anhu kua:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ وَاللَّفْظ لَهُ قَالَ حَدَّثَنَا أَبُو خَالِدٍ الْأَحْمَرُ عَنْ ابْنِ عَجْلَانَ عَنْ عَامِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ الزُّبَيْرِ عَنْ أَبِيهِ قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا قَعَدَ يَدْعُو وَضَعَ يَدَهُ الْيُمْنَى عَلَى فَخِذِهِ الْيُمْنَى وَيَدَهُ الْيُسْرَى عَلَى فَخِذِهِ الْيُسْرَى وَأَشَارَ بِإِصْبَعِهِ السَّبَّابَةِ وَوَضَعَ إِبْهَامَهُ عَلَى إِصْبَعِهِ الْوُسْطَى وَيُلْقِمُ كَفَّهُ الْيُسْرَى رُكْبَتَهُ

Amesema Abu Bakr Ibn Abi Shaybah kua amesema Abu Khalid al Ahmaru kua amesema Ibn Aajilani kua amesema Amiri Ibn Abd Allah Ibn Zubayr kua amesema Babayake kua: 'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alipokua akisali, basi alikua akikaa na kuomba huku mkono wake wa Kulia Ukiwa juu ya Paja la Kulia, Mkono wake wa kushoto ukiwa juu ya Paja la Kushoto, alikua akinyoosha Kidole chake cha Shahada kwa kuweka kidole chake cha Gumba kwenye Kidole chake cha kati, na mkono wake wa Kushoto ukiwa juu ya Goti la Kushoto*(Sahih Musim)*

Naam hii ni hadith nyengine ya Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu*aliyoielezea Mtoto wake aitwae Amir, ambayo ni yenye kuthibitisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua ni mwenye kunyoosha kidole cha shahada, baada ya ile hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu.*

Ambapo ndani yake inasema kua *Rasul Allah Salallahu Allahu Alayhi wa salam* alipokua Akisali basi anapokaa Kitako hua ni mwenye kuomba Dua, Ambapo Dua hii hapa haijakusudiwa kitu chengine chochote isipokua Tahiyyat, na Abd Allah Ibn Zubayr ameiita Dua kwa sababu maana nyengine ya Tahiyyat hua ni Dua na vile vile ndani yake mna kuombeana Usalama kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kwa Mwenye kusali na pia kwa Waja wema.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anapokaa Tahiyyat basi hunyoosha mikono yake. **Kuelekea mwishoni mwa Mapaja yake Na hivyo mkono wa wa kulia hushika paja la Kulia karibu na Goti na mkono wa kushoto paja la kushoto karibu na Goti.Hivyo ni Muhimu katika mkao wa Tahiyyat kwa ncha za vidole vya Mikono kufikia kwenye Magoti.**

Kwani katika Hadith ya Wail Ibn Hujayr *Radhi Allahu Anhu* pia iliyopo katika Sunnan An Nasai Ni mwenye kusema kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiweka kisugudi cha Mkono wake wa Kulia kwenye Paja la kulia na Mkono wa kushoto juu ya goti la kushoto.'**

Ambapo kwa mkao huu ndio itakua inawezekana kwa ncha za Vidole kua ni zenye kugusa Magoti.Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi kua: '**Wanazuoni ni wenye kukubaliana kua inapendekezwa kuweka viganja vua Mikono kwenye Goti au Juu ya Goti, na kuna wanaosema kua Vidole vinatakiwa vijikunje kwenye goti kama kwamba ni vyenye kulikamata Goti husika na hii hua ni katika Tahiyyat ya Kwanza na ya Pili ambapo Mkunjuo wa kidole cha Shahada na unyooshaji wake hua unajulikana pia kama Tasbiha.**

Na amesema tena Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:

: أن رسول الله صلى الله عليه وسلم كان إذا قَعد في التَّشهد وضع يَده اليُسرى على رُكْبَتِه اليُسْرَى، ووضع يَده اليُمنى على رُكبته اليُمنى، وعَقَد ثلاثة وخمسين وأشار بالسَّبَّابة".

‘Katika kila wakati ambao *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akikaa kwa ajili ya Tashahhud, basi alikua akiweka Mkono wake wa kushoto juu ya Goti la Kushoto na akiweka Mkono wake wa kulia juu ya Goti la Kulia na kufanya nambari 53 kwa kunyoosha Kidole chake cha Shahada.’

Na amesema Wail Ibn Hujwayr *Radhi Allahu Anhu* katika Sunan Abu Daud kua:

ثم جلس فافترش رِجله اليُسرى، ووضع يَده اليُسرى على فخذه اليسرى، وحَدَّ مِرفقه الأيمن على فَخذه اليَمنى، وقَبِض ثنتين وحَلَّق حَلَقة، ورأيته يقول هكذا، وحَلَّق بِشْرٌ الإبْهَام والوُسْطَى وأشار بالسَّبَّابة".

Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hukaa kitako na kuusogeza mbele Mguu wake wa Kushoto, na huweka Mkono wake wa Kushoto kwenye Paja la kushoto na Kisugudi chake cha Kulia kwenye Paja la Kulia na kisha hufunga Ngumi na kuifanya Duara, nami nimemuona kama hivi. Kisha Bishr akakunja Ngumi na kufanya alama ya duara baina ya Kidole Gumba na Kidole cha kati huku Akiwa ni mwenye kunyoosa Kidole cha Shahada.

Ambapo Anasema Mujaddid Ad Din, Shaykh ul Islami Al Hafidh Imam Abu Fadhl Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Asqallani A Shafii kua: ‘**Baadhi ya wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* alikua Akifanya hivyo mwanzoni tu mwa kikao chake cha Tahiyyat kama ilivyoainiahwa na baadhi ya Hadith.’**

Na tunapoangalia Hadith hizi tunaona kua ndani yake hakuna hadith iliyosema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitikisa Kidole chake cha Shahada katika wakati wa kusoma Tahiyyat.

Kwani hadith zinasema tu kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akinyoosha Kidole chake cha Shahada. Ambapo kitendo hiki cha Kunyoosha kidole bila ya Kukitikisa au kukichezesha katika wakati wa Tahiyyat hua pia kunaashiria kujumuisha Tawhid katika Maneno, Vitendo na Imani.

Na katika Hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* iliyonukuliwa na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi tunaona kua yeye amesema kua:

"لهي أشدُّ على الشيطان من الحديد".

‘Kunyoosha kidole huko hua ni kwenye kuonesha Ukali madhubuti sana dhidi ya Shaytan kuliko Umadhubuti wa Chuma.’

Ambapo katika Hadith hizi pia tunaona kua Katika kukaa kwake Tahiyyat *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* alikua akishika Goti kake kwa mkono wa kushoto.Na pia baadhi ya wakati alikua akiwrka tu mkono wake juu ya Goti bila ya Kupindisha vidole kama kwamba amelishika goti lake hilo.Kwa maana hio basi hai zote mbili hizi hua zinaruhusika kuhusiana na Ukaaji wa Mkono wa kushoto katika Goti la Kushoto katika Tahiyyat.

Hivyo kulingana na vithibitisho vya Hadith tulizoziangalia basi tunaona kua Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanasema kua hua ni Sunna kuashiria Shahada ya Tashshahud kwa kunyoosha kidole cha Shahada cha Mkono wa Kulia ambacho hua kinatakiwa kinyooshwe katika wakati wa kusema maneno *Illa Allah.*

الا الله

Ambapo hio ni kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii.

Na kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Al Muhaqqiqin Al Faqih Al Hafidh Imam Abu Fadhl Shihab Ad Din Ahmad Ibn Hajar Al Haitami basi yeye anasema kua: '**Kidole cha Shahada katika Tashshahud kinatakiwa Kinyooshwe katika wakati wa kuanza kutamka herufi Hamza ya neno Illa Allah.'**

Ambapo kwa upande wa Al Hafidh Al Imam Al Khatib Al Shibrini Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Katika wakati Ambao kidole kinanyoshwa basi hua ni Sunnah pia kidole hicho Kisielekee Juu bali kipinde kidogo kuelekea chini katika Upande wa Kibla huku mhusika akiwa na nia ya Kuashiria Tawhid ya kumpwekesha *Allah Subhanah wa Ta'ala*** *' (Tuhfah Al Muhtaj bi sharh al Minhaj 3/70 na Al Mughni Al Muhtaj 1/378)*

Kwani tunapowaangalia Wanazuoni wengine Mahiri Sulayman wawili wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ni Imam Sulayman Al Jamal ambae ni muandishi wa *Hashiyyah Al Jamal Ala Sharh Al Minhaj*ambayo ni ufafanuzi wa *Tuhfah al Muhtaj* ya Imaam Ibn Hajar Al Haytami na Imam Sulayman Ibn Muhammad Al Bujairimi ambae niMwandishi wa *Hashiyyah Al Bujairimi Alaa Al Khatib* ambayo ni ufafanuziwa Sharhya Imam Al Mughni ya Al Shiribini na hivyo wote kua ni Waandisha wa vitabu viwili vya Hashiyyah yaani Ufafanuzi wa Kina wa Mitizamo ya Kifiqh katika Madhhab ya Imam Al Shafii kwani Hashiyyah hua ni Ufafanuzi wa vitabu vya Sharh ambayo Waswahili wanasema Sherehesho.

Basi Maimam Sulaiman wawili hawa wanasema kua: '**Katika wakati wa Kutoa Shahada ndani ya Tashshahud ya Sala basi Mtu anatakiwa Anyooshe kidole cha Shahada cha Kulia kama *Tahqiq* (Hakikisho la Shahada) kuanzia katika wakati wa kutamka maneno *Illa Allah*, na kisha kidole hicho hua hakitakiwi kushushwa hadi katika wakati wa kunyanyuka na kuja juu kama ikiwa ni katika Tahiyyat ya Mwanzo na kama ikiwa ni katika Tahiyyat ya Mwisho basi kidole kinyooke hadi katika wakati wa kutoa Salam.'**

Ama kwa upande wa Imam Abd Rahman Al Jazari ambae ni Mwandishi wa Kitabu cha *Al Fiqh Ala Al Madhahib Arbaa* basi anasema kihusiana na Mitizamo ya Madhhab Manne kuhusiana na Kunyooha Kidole cha Shahada katika Tahiyyat kua: '**Wanazuoni wa Madhhab wametofautiana kuhusiana na Kunyoosha Kidole cha Shahada katika Tahiyyat kwa Mitizamo ifuatayo:**

Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua:'Mtu anatakiwa Anyooshe kidole chake cha Shahada tu, na hivyo kama ikiwa anatatizo katika Kidole chake hicho, labda maradhi au haiina uwezo wa kinguvu kusimama basi Mtu huyo hatotakiwa kunyoosha kidole hicho wala kidole chengine chochote kile. Na kidole kinatakiwa Kinyooshwe katika wakati wa Kutamka neno 'La' ambalo ni lenye kukanusha katika maneno *La Ilaha Illa Allah.*

Kidole hicho kitasimamishwa hadi mwisho wa maneno hayo, yaani Kidole hunyooshwa katika Kuthibitisha tu kwa maneno kua 'La Ilaha Illa Allah' na kisha baada ya kumaliza maneno hayo basi hua haina haja kunyoosha kidole.

Na hivyo kidole hicho cha Shahada kitalazwa, ambapo Kunyoosha kidole huko humaanisha Kukanusha Kua 'La Ilaha' na kukilaza kwake baada ya 'Illa Allah' hua ni kuthibitisha kua Isipokua Allah.'

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua:'Katika Wakati wa Kukaa Tahiyyat Basi Mtu anatakiwa Afunge ngumi Mkono wake wa Kulia huku akiwa ni mwenye kunyoosha Kidole cha Shahada kwa kukisimamisha na Kukilaza taratibu tangu mwanzo wa Tahiyyat Hadi Mwisho.'

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua:'Katika Kukaa Mkao wa Tahiyyat basi Mtu anatakiwa akunje kidole chake kidogo na kidole cha Pete huku akiwa ni mwenye Kuvinyoosha vidole vitatu vilivyobakia na kisha katika wakati wa kutoa Shahada basi Mtu anatakiwa kunyoosha kidole cha Shahada hadi mwisho wa Tahiyyat.''

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Imam Al Jazari amesema kama tulivyoelezana hapo kabla, kama alivyosema Imam An Nawawi.Isipokua Imam Al Jazari ameongezea kuhusiana na Mtizamo wa Imam Al Shafii kwa kusema kua: '**Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kua Mtu anaponyoosha kidole cha Shahada basi hua anatakiwa kukiangalia Kidole hicho hadi amalize Kisomo cha Tahiyyat yake hio.'**

Kwani amesema *Shaykh Ul Islami* Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Hua ni Sunna kutouondoa Mtizamo wa Macho yako katika Kidole cha Shahada, kwani kuna Hadith sahih kuhusiana na Jambo hili katika Sunan Abu Daud'***(Sharh Sahih Muslim)*

Kwani anasema *Al Hafidh, Al Faqih* Imam Abu Bakr Ahmad Ibn Husayn Ibn Ali Ibn Musa Ibn Khusrawjidi Al Bayhaqi Al Shafii kua; '**Mmoja kati ya Watu wa Madina alisema kua: Siku Moja mimi nilisali pembeni ya Khifaf Ibn Imaa Ibn Rukhsa *Radhi Allahu Anhu,* na baada ya Kuniona nikiwa nnanyoosha Kidole katika Tahiyyat.Basi akaniambia: 'Ya Akhi! Hivi kwanini ulinyoosha Kidole?.'**

Ambapo nami nikajibu: 'Kwa Sababu mimi nimewaona Wabora miongoni mwa Watu na Wanazuoni wakifanya Hivyo.'

Ambapo nae akasema: 'Naam Uko Sahih kwani mimi Nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akinyoosha Kidole chake cha Shahada katika Wakati alipokua amekaa Tahiyyat ndani ya Sala.Na hivyo Makafiri walipomuona akifanya Hivyo basi wakamtuhumu kua anawaroga, lakini walikua Waongo, kwani ukweli ni kua *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam* alifanya hivyo kwa ajili ya Kushuhudia Umoja na upekee wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.'(Sunnan Al Kubra)*

Ama tunaporudi katika kuangalia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Kunyoosha kidole katika wakati wa kutamka *Illa Allah.*Basi Imam Al Bayhaqi amesema katika Hadith nyengineyo kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema huku akiashiria kwenye Kidole chake cha Shahada kua: Hiki kinamaanisha Ikhlas**. **Na huu (Huku akinyanyua Mkono wake) Hua Unamaanisha Duaa**. **Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyua Mkono juu zaidi na kusema:Na hivi hua inamaanisha *Ibtihal* (Maombi makubwa zaid**)*'(Sunan Al Al Kubra)*

Na akasema tena Imam Al Bayhaqi na Imam Abu Bakr Ibn Abi Shaybah kua: '**Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Kunyoosha Kidole cha Shahada hua ni Ikhlas(yaani katika kusema *Illa Allah***'*(Sunan Al Kubra)*

Na Imam Ibn Abi Shaybah amesema kua: '**Amesema Imam Ibrahim An Nakhai kua, Inapendekezwa Kunyoosha Kidole katika Wakati wa Kutoa Shahada katika maneno *Illa Allah* kwa sababu hua ni Tawhid, na hua inakirihisha kunyoosha Vidole viwili.'**

Ambapo anasema Imam Abu Muhammad Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Farraa Al Baghawi Al Shafii kua: '**Watu wa Kizazi cha Tabiina walikua wakinyanyua Kidole chao cha Shahada katika Tahiyyat pale wanapotamka meneno Illa Allah, na Wengi sana miongoni mwa Wanazuoni wa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na waliofuatia na Waliofuatia pia walikua wakifanya hivyo hivyo kunyoosha Vidole vyao katika Tahiyyat katika wakati wa maneno Illa Allah.'**(*Sharh Al Sunna)*

Naamesema Abd Allah Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akikaa Tahiyyat alikua akiuweka Mguu wake wa Kushoto baina ya mapaja yake na ugoko wake wa mguu wa kulia ambao huukalia. Na kisha huweka mkono wake wa kushoto juu ya Goti ka kushoto na kisha huweka mkono wake wa kulia juu ya Paja la kulia, na kisha Hunyoosha kidole, na alikua akinyoosha kidole anaposoma Tahiyyat bila ya kutikisa kidole***(Imam Abu Daud)*

Na amesema tena Imam Abu Daud kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ، حَدَّثَنَا يَحْيَى، حَدَّثَنَا ابْنُ عَجْلَانَ، عَنْ عَامِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ الزُّبَيْرِ، عَنْ أَبِيهِ، بِهَذَا الْحَدِيثِ، قَالَ: لَا يُجَاوِزُ بَصَرُهُ إِشَارَتَهُ . وَحَدِيثُ حَجَّاجٍ أَتَمُّ

Amesema Muhammad Ibn Bashar kua, amesema Yahya kua:Amesema Ibn Ajlankua amesema Amer *Ibn Abd Allah Ibn Zubayr Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na hadith hii kua na inatakiwa Mtizamo wa Macho usivuke ishara ya kidole hicho cha Shahada*(Sunna Imam Abu Daud)*

Kwani kwa upande wa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik ambao wao hua ni wenye kutikisa kidole katika wakati wa kutoa shahada basi wanasema kua: '**Amesema Imam Abu Zayd Al Qayrawani kua: Amesema Ibn Al Qasim kua: 'Hakika mimi nimeuona Malik akichezesha kidole chake katika wakati wa Tashshahud bila kukituliza. Na katika wakati anapoomba Dua hunyanyua mikono yake na hivyo kiganja chake hua kinaangalia Uso wake**. **Na Yahya Ibn Muzayn amesema kua: Kidole cha Shahada kinyanyuliwe kiasi ya kua Upande wake waa kushoto uwe unakabiliana na Uso, na hakitakiwi Kutikiswa***(An Nawadir wa Ziyadah)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Baji basi yeye anasema kua: '**Inaoneka kua kutikisa kidole cha Shahada hua kunampelekea mtu kua na Umakini kunakopelekea kumdhibiti shaytan, ambapo katika kutikisa kidole huko humpelekea mtu kuani mwenye kukumbuka kua yuko ndani ya Sala,na Imam Malik alikua akifanya hivyo katika Tahiyyat.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Ibn Al Qasim basi yeye amesema kua: '**Mtu mwenye kusali na kusoma Tahiyyat basi anatakiwa kunyoosha kidole cha shahada bila ya kukitikisa, huku akiufanya upande wa kushoto wa kidole hicho kua ni wenye kuangalia juu**. **Ama mtizamo ulioeleezewa na Imam Yahya Ibn Maryam wakutikisa kidole hua unatafsirika kua ni sehemu ya kuleta umakini ndani ya Sala na Kumdhibiti Shaytan.'**

'Ambapo wale aanaosema kua haitakiwi kukitisa basi hua ni wenye mtizamo wa kua kufanya hivyo hua ni kuashiria Tawhid. **Na imenukuliwa na Yahya kua Ibn Umar alikua akitikisa kidole**

katika wakati asemao *Ashhadu An Lailaha illa Allah wahdahu la sharika lah* na hii labda alikua akimaanishakukinyoosha bila kukitikisa,wa *Allahu Aalam*.'

JEE TAHIYYAT YA MWANZO NI WAJIB AMA SUNNAH?

❖❖❖

Kwani tunapoangalia kuhusiana na Umuhimu wa Tahiyyat ya Mwanzo katika Sala ili kuweza kujibu Suali la kua ni Wajib ama la, basi tunaona kua juu ya Suali hili kuna mitizamo miwili tofauti kulingana na Wanazuoni.

Ambapo mtizamo wa Kwanza ni Mtizamo wa Wanazuoni wasemao kua Tahiyyat ya Mwanzo hua ni Wajib, na hivyo kama Mtu anaesali akiiwacha kwa Makusudi basi Sala ya Mtu huyo hua ni Batili,na kama Mtu akiiwacha kwa Kusahau basi hua ni Wajibu wa Mtu husika alieisahau kufanya Sijdat Sahw na hivyo Sala yake itakua ni Sahih.

Na huu ni Mtizamo wa Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Abu Tahwr Al Shafii, Imam Is-haq Ibn Rahawayh Al Shafii na Imam Abu Daud.Ambapo wao kuhusiana na Mtizamo wao huu basi wanasimamia kwenye Uthibitisho wa Hadith ya Rifah *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na ukamilifu wa Sala kua:

فَإِذَا جَلَسْتَ فِي وَسَطِ الصَّلاَةِ فَاطْمَئِنَّ وَافْتَرِشْ فَخِذَكَ الْيُسْرَى ثُمَّ تَشَهَّدْ ثُمَّ إِذَا قُمْتَ فَمِثْلَ ذَلِكَ حَتَّى تَفْرُغَ مِنْ صَلاَتِكَ ''

Na unapokaa kitako katikati ya Sala basi kamilisha kikao na kisha tanua Paja lako la Kushoto na Usome Tahiyyat,na unaposimama tena Fanya hivyo hivyo hadi utakapomaliza Sala yako*(Sunan Abu Daud)*

Na pia katika Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:Anaposali mmoja wenu na kisha akakaa kitako ndani yake basi na Asome *Tahiyyat Lillah**i.'(Imam Abd Al Ghani Al Maqdisi Ibn Qudamah)***

Kwani baada ya Mtizamo huo basi kuna Mtizamo usemao kua: **'Tahiyyat ya Mwanzo ya Sala hua ni Sunnah.'**Ambapo huu ni Mtizamo wa wengi sana Miongoni mwa Wanazuoni,Akiwemo Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Sufyan Ath Tahwry, Imam Abu Hanifa, Imam Malik Ibn Anas, Imam Al Awzai na kadhalika.

Na Wanazuoni wenye Mtizamo huua wao ni wenye kusimamia Uthibitisho wa Hadith ifuatayo:

أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم صَلَّى بِهِمُ الظُّهْرَ فَقَامَ فِي الرَّكْعَتَيْنِ الأُولَيَيْنِ لَمْ يَجْلِسْ.

Amesema Abd Allah Ibn Buthaynah *Radhi Allahu Anhu* kua: Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha Sala ya Adh Dhuhr. Na kisha akasimama baada ya Sijda ya Rakaa ya pili na hakukaa Tahiyyat,lakini baada ya Kumaliza kusali Akasujudu mara mbili Sijdat Sahaw.'

Yaani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliifidia Tahiyyat ya kwanza kwa Sijdat Sahw,hivyo kama ingekua si Sunnah basi asingeifidia, kwani Sijdat Sahw hua haiwezi kufidia kitu ambacho ni Wajib.

Hivyo kwa upande wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii basi kisomo cha Tahiyyat ya Mwanzo hua ni Sunna inayotiliwa mkazo.Na kutokana na kua ni Sunnah inayotiliwa mkazo basi hua pia inahimizwa kuleta Sijdat Sahaw kama ikiwa Mtu ataisahauTahiyyat ya Kwanza. Ambapo hata hivyo pia hua hakuna ulazima wa Kuleta Sijdat Sahw kama Mtu ataisahau Tahiyyat ya kwanza.

Na hapa inabidi pia tufahamiane kua Sijdat Sahaw hii hapa pia hua ni Sunnah katika Madhhab ya Imam Al Shafii kama tutakavyofafanua hapo baadae Inshaa Allah.Lakini hata hivyo Sijdat Sahw hua ni Wajib kwa Mtu mwenye kumfuata Imam ambae atatekeleza Sijdat Sahw Na hii ni kwa Sababu Haikubaliki kupingana na Imam Katika Sala.Hivyo kuvunja Nguzo ya Sala hua ni kwenye kuelekea kuifanya Sijda Sahw kua ni Wajib kutekelezwa.*(Al Mutamad, Imam Al Zuhayly)*

Na kwa maana hio basi kwa kua Tunazungumzia kuhusiana na Tahiyyat ya kwanza ambayo ni Sunna katika hali ya kua ni iliyosahauliwa, basi hata kama Mtu akisahau Tahiyyat ya kwanza na kisha akasahau kuleta Sijdat Sahw basi Sala yake hua haijabatilika.

Kwani kama itatokea kua Mtu ametoka kwenye Sijda ya Rakaa ya Pili na kisha akanyanyuka kabla ya Kukaa Tahiyyat, lakini kabla hajafika juu na kusimama sawia akakumbuka kua kumbe hajakaa Tahiyyat ya kwanza, basi Mtu huyo humbidi kurudi na kukaa Tahiyyat.

Lakini kama ikiwa amekumbuka wakati tayari ameshasimama basi hua hawajibiki kurudia chini kukaa Tahiyyat na hii ni kwa sababu Kisimamo hua kinahesabika ni Nguzo ya Sala.Na Tahiyyat inahesabika kua ni Sunnah inatiliwa mkazo, basi hua hairuhusiki kuvunja nguzo kwa sababu ya Sunnah.

Ambapo kwa Upande wa Imam Ibn Abidin Al Shami Al Hanafi basi anasema kua: '**Tahiyayat ya kwanza sio Fardhi bali ni Wajib**. **Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Vitendo ambavyo ni Wajib ambavyo Mtu anaesali atakua amevikosea au hakuvitekeleza basi Sala yake Mtu huyo hua haibatiliki isipokua hua ni yenye kua na kasoro. Na kutokana na kua ni yenye kasoro basi hua ni Wajib kuirudia Sala hio mara tu baada ya kumaliza, au ndani ya wakati wake**. **Ambapo kama itakua wakati wake umeshapita basi Wajibu huo wa kuirudia Sala hio hua hauondoki, na hii ni kulingana na baadhi ya Wanazuoni, ambapo kwa baadhi ya Wanazuoni wengine basi hua wanasema kua hua si wajib bali hua inapendekezwa.'***(Rad Al Mukhtar)*

KISIMAMO BAADA YA TAHIYYAT YA PILI

❖❖❖

Naam..mara baada ya kumaliza kusoma Tahiyyat kitendo kinachofuatia hua ni kusema Allahu Akbar na kisha moja kwa moja kunyanyuka na kusimama huku ukinyanyua juu mikono kama ifanywavyo mwanzoni katika wakati wa Kufunga Sala.

Kwani amesema Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu kua:'**Wakati Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alipokua akitamka Takbirat Al Ihram basi alikua akinyanyua Mikono yake kukabiliana na Mabega yake. Na anaporukuu hufanya hivyo na anaponyayuka kutoka katika Rukuu kuelekea kwenye Sijda basi hufanya hivyo, na anaponyanyuka kutoka katika Tahiyyat ya pili basi hufanya hivyo.'***(Sunan Abu Daud)*

Na amesema Imam Nafii mawla Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Katika kila wakati ambao Ibn Umar Radhi Allahu Anhu alipokua akianza Sala yake kwa Takbir Al Ihram basi alikua akinyanyua mikono yake, na kila anaporukuu basi hunyanyua mikono yake na pale anaposema Sami Allahu Liman Hamida Hunyanyua Mikono yake, na anaponyanyuka kuingia kwenye Rakaa ya Tatu hunyanyua mikono yake. Na Ibn Umar mwenyewe alikua akisema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifanya hivyo pia.'**

Ambapo amesema Shaykh ul Islami Imam Ibn Daqiq Al Idd al Shafii kua: **'Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua: Inapendekezwa kunyanyua mikono katika Sala kwa sababu kuna Vithibitisho juu yake. Kwani kuna uthibitisho wa Kunyanyua mikono katika Wakati wa kuingia kwenye Sala, kuna uthibitisho wa kunyanyua Mikono katika wakati wa Kurukuu, kuna uthibitisho wa kunyanyua Mikono katika wakati wa Kuelekea chini kwenye Sijda na pia kuna Uthibitisho wa Kunyanyua mikono katika wakati unaposimama kutoka katika Rakaa ya pili kuinhia katika Rakaa ya Tatu.'**

'Na jambo hilo pia limeridhiwa na Vizazi vya Mwanzoni vya Uislam na vya wale waliokua wakifanya hivyo hapo kabla yaa vizazi vya Mwanzoni kwani Hadith zimethibitisha juu ya jambo hilo. Ambapo baada ya kuja juu nakusema Allahu Akbar huku ukiwa umenyanyua juu mikono na kisha kuifunga, basi unakua umeshaingia katika Rakaa ya Tatu na kinachofuatia hua ni kusoma Surat Al Fatiha.'

Kwani anasema Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* alipokua akisimama kusali Sala za Fardhi basi alikua akisema Allahu Akbar na Hunyanyua Mikono yake hadi mikono hio kukabiliana na mabega yake.Na hufanya Hivyo hivyo mara baada ya kumaliza kisomo cha Qur'an pale anapotaka kurukuu, Na hufanya hivyo hivyo pale anapotoka kwenye kurukuu. Na hakufanya hivyo katika wakati akiwa amekaa kitako kwenye kikaoi cha Sala.Na anaposimama kutoka kwenye Sijda (mwishoni mwa rakaa ya pili baada ya Tahiyyat) hua ni mwenye kunyanyua Mikono yake huku akisema Allahu Akbar'***(Sunan Abu Daud, Musnad Imam Ahmad, Sunnan Ibn Majah, Sunnan At Tirmidhii)*

Hivyo kama tulivyosema hapo kabla kua kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua ni Sunna inayopendekezwa kunyanyuka kama vile mtu anaponyanyuka kutoka kwenye Jalasat Al Istiraaha.Yaani kwa kunyanyuka huku ukiwa unategemea Ardhini kwa mikono yako kwa sababu ndio njia yenye kuonesha unyenyekevu zaidi.Ambapo Rakaa ya Tatu hua ni sawa na Rakaa ya kwanza, isipokua katika Rakaa ya Tatu na ya Nne pia hua haitakiwi kusoma Sura nyengine yeyote ile isipokua Surat Al Fatiha tu.

Kwani amesema Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Baba yangu amesema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Surat Al Fatiha na kufuatishia na nyenginezo katika Rakaa mbili za Mwanzo za Sala. Na alikua akisoma Surat Al Fatiha tu peke yake katika Rakaa mbili za Mwisho za Sala ya Adhuhuri. Baadhi ya Wakati ilikua unasikia baadhi ya Aya, na alikua akirefusha Rakaa mbili za mwanzoni zaidi kuliko mbili za mwishoni naalikua akifanya hivyo katika Sala ya Al Asr na Alfajr pia***.'(Sahih Bukhari)*

Hivyo katika Rakaa ya Tatu baada ya kusoma Surat Al Fatiha basi Unarukuu na Kusjudu kukamilisha Rakaa, na hivyo kama Mtu anasali Sala ya Rakaa Tatu kama Maghribi, basi baada ya Sijda ya pili ya Rakaa ya Tatu atasoma Tahiyyat ya Mwisho.

Lakini kama ni Sala ya Rakaa nne basi kama Salat Dhuhr basi baada ya Sijda ya pili ya Rakaa ya Tatu atakuja juu tena ambapo katika Takbira yake hii hatonyanyua Mikono yake.Kisha atakamilisha Rakaa ya nne kwa kwa kukaa kitako katika kikao cha Tahiyyat ya mwisho.

11-KIKAO CHA TAHIYYAT YA MWISHO.

❖❖❖❖

Anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Kusoma Tahiyyat ya Mwisho na Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani yake hua ni Nguzo ya Sala**. **Ingawa Kufanya hivyo katika Tahiyyat ya Kwanza hua ni Sunna***(Al Majmuu)*

Kama inavyoelezeaa Hadith ifuatayo:

حَدَّثَنَا مَحْمُودُ بْنُ غَيْلاَنَ، حَدَّثَنَا أَبُو دَاوُدَ، - هُوَ الطَّيَالِسِيُّ حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، أَخْبَرَنَا سَعْدُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، قَالَ سَمِعْتُ أَبَا عُبَيْدَةَ بْنَ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ، يُحَدِّثُ عَنْ أَبِيهِ، قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم إِذَا جَلَسَ فِي الرَّكْعَتَيْنِ الأُولَيَيْنِ كَأَنَّهُ عَلَى الرَّضْفِ . قَالَ شُعْبَةُ ثُمَّ حَرَّكَ سَعْدٌ شَفَتَيْهِ بِشَيْءٍ فَأَقُولُ حَتَّى يَقُومَ فَيَقُولُ حَتَّى يَقُومَ . قَالَ أَبُو عِيسَى هَذَا حَدِيثٌ حَسَنٌ إِلاَّ أَنَّ أَبَا عُبَيْدَةَ لَمْ يَسْمَعْ مِنْ أَبِيهِ . وَالْعَمَلُ عَلَى هَذَا عِنْدَ أَهْلِ الْعِلْمِ يَخْتَارُونَ أَنْ لاَ يُطِيلَ الرَّجُلُ الْقُعُودَ فِي الرَّكْعَتَيْنِ الأُولَيَيْنِ وَلاَ يَزِيدَ عَلَى التَّشَهُّدِ شَيْئًا . وَقَالُوا إِنْ زَادَ عَلَى التَّشَهُّدِ فَعَلَيْهِ سَجْدَتَا السَّهْوِ . هَكَذَا رُوِيَ عَنِ الشَّعْبِيِّ وَغَيْرِهِ

Amesema Muhammad Ibn Ghaylani, kua amesema Abu Daud ambae ni At Tayalisi kua amesema Shu'bat kua amesema Said Ibn Ibrahim kua nimemsikia mimi Abu Ubaydah Ibn Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua:Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akikaa kwenye Rakaa mbili za Kwanza (Kwenye Tahiyyat ya kwanza) ilikua kama Mtu aliekaa kwenye Mawe ya Moto.'*(Imam At Tirmidhii)***

Hivyo maneno yasemayo 'Kama aliekaa kwenye Mawe ya Moto' yanamaanisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisimama mara tu baada ya Kushuhudia na Salat An Nabii katika Tahiuyat ya kwanza. **Na ingawa Hadith hii ni dhaifu kutokana na kua ni yenye kukosa kiunganisho cha baina ya Abu Ubaidah na Baba yake.**

Lakini pia kwa upande mwengine tunaona kua Hadith hii imenukuliwa pia na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* na Umar Ibn Al Khattab pia *Radhi Allahu Anhu.*Na imenukuliwa katika Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal, Sunnan Abu Daud, Sunan An Nasai, Sunan Ibn Majah na Sunnan At Tirmidhi.

Na Imam At Tirmidhii amesema kua hii ni Hasan Hadith na kusema kua: '**Ingawa Abu Ubaidah Ibn Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* hakusikia Hadith kutoka kwa Baba yake, lakini Wanazuoni wanaitumia Hadith hii na kuifanyia kazi katika kupendekeza kwa Mtu anaesali kua**

asikae kitako sana katika Tahiyyat ya kwanza, na pia asiongeze kitu chengine chochote katika Tahiyyat baada ya Shahada na Salat An Nabii tu.'

Ambapo mtizamo wa kua Salat An Nabii Katika Tahiyyat ya Mwanzo hua ni Sunna inayopendekezwa kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Ibn Hubayrah, Imam Al Ajurri na Imaam Ibn Hazim, mbali ya kua Wanazuoni wa Madhhab mengine wao wanasema kua Salat An Nabii hua haina ulazima kwani unaweza kumalizia Tahiyyat yako mara baada ya kutoa Shahada tu.

Kwani anasema Imam Al Khatib Al Shirbini kua: '**Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya mwisho inayofuatiwa na Taslim (kutoa Salam) hua ni Fardhi hata kama ikiwa Sala husika haijajumuisha Tahiyyat ya Kwanza kwa mfano kama Sala ya Al Fajr.'**

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: **'Kusoma Tahiyyat ya Mwisho na Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani yake hua ni Nguzo ya Sala**. **Ingawa Kufanya hivyo katika Tahiyyat ya Kwanza hua ni Sunna.'***(Al Majmuu)*

Kisha Imam An Nawawi anaendelea kutuambia kua: **'Kwani amesema Ubaidah Ibn Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua:Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua anapokaa kwenye Rakaa mbili za Kwanza (Kwenye Tahiyyat ya kwanza) ilikua kama Mtu aliekaa kwenye Mawe yamoto.'** *(Imam At Tirmidhii)*

Hivyo maneno yasemayo 'Kama aliekaa kwenye Mawe ya Moto' yanamaanisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisimama mara tu baada ya Kushuhudia na Salat An Nabii katika Tahiyyat ya kwanza.Na ingawa Hadith hii ni dhaifu kutokana na kua ni yenye kukosa kiunganisho cha baina ya Ubaid Allah na Baba yake.

Lakini pia kwa upande mwengine tunaona kua Hadith hii imenukuliwa pia na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* na Umar Ibn Al Khattab pia *Radhi Allahu Anhu.*

Na imenukuliwa katika Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal, Sunnan Abu Daud, Sunan An Nasai, Sunan Ibn Majah na Sunnan At Tirmidhi.Na Imam At Tirmidhi amesema kua hii ni Hasan Hadith na kusema kua: 'Ingawa Ubaid Allah Ibn Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* hakusikia Hadith kutoka kwa Baba yake, lakini Wanazuoni wanaitumia Hadith hii na kuifanyia kazi katika kupendekeza kwa Mtu anaesali kua asikae kitako sana katika Tahiyyat ya kwanza, na pia asiongeze kitu chengine chochote katika Tahiyyat baada ya Shahada na Salat An Nabii tu.'

Kwani anasema Imam Al Khatib Al Shirbini kua:'**Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat inayofuatiwa na Taslim hua ni Fardhi hata kama Sala husika itakua haina Tahiyyat ya kwanza kama Sala ya Al Fajr kwa mfano**. **Lakini Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni ni kua Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya kwanza basi hua ni Sunnah Lakini hata hivyo Mtizamo Sahih miongoni mwa Wanazuoni kuhusiana na kuitumia Salam Familia ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya mwanzo hua si Sunnah kama ilivyoonesha Hadith iliyotajwa hapo kabla.'***(Al Mughni)***

Kwani kwa upande wa Sunan Imam At Tirmidhi Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Abu Daud, basi kuna hadith ya Ibn Ubayd *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: '***Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*alimsikia Mtu akisali na kuomba Dua huku akiwa hajasoma Salat Nabii, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Mtu huyu amefanya haraka'**

Na kisha akamuita Mtu huyo na kumwambia: 'Mmoja wenu anaposali na kuomba dua basi na aanze na kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala na* kisha kufanya Salat Nabii na kisha ndio aombe kitu chochote anachokitaka.'

Hivyo kama tulivyoona katika Tahiyyat ya Mwanzo kua mwisho wake hua ni Katika Kushuhudia na Salat Nabii tu, na kisha unafanya Takbir huku ukinyanyua mikono yako na unanyanyuka na kusimama kuingia kwenye Rakaa ya Tatu.

SALAT IBRAHIMIYYAH NA MANUFAA YAKE

❖❖❖

Katika kisomo cha Tahiyyat ya Mwisho basi hua ni yenye kuongezewa kumalizia kwa Salat Ibrahimiyyah, yaani Sala ya Kumsalia Muhammad *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na pia *Khalillu Allah Ibrahim Alayhi Salatu wa Salam* kwa kusema:

التَّحِيَّاتُ الْمُبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ الطَّيِّبَاتُ لِلَّهِ سَلاَمٌ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ سَلاَمٌ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ أَشْهَدُ أَنْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ

اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ عَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ وَ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ عَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

At Tahiyyatu, Al Mubarakatuh, As Salawatu Al Tayyibatu Lillahi Salamu Alayka Ayyuha Nnabiyu wa Rahmat Allahi wa Barakatuh, Asalamu Alayna wa Aala Aibadi Allahi Salihina, Ashhadu An Lailaha Illa Allah wa Ashhadu AnNa Muhammadan Rasul Allah.

Allahumma salli `ala Muhammadin wa `ala ali Muhammadin kama sallaita `ala Sayyidina Ibrahima wa `ala ali Ibrahima Innaka hameedun Majid Allahumma barik `ala Muhammadin wa `ala ali Muhammadin kama barakta `ala Ibrahima wa `ala ali Ibrahima Innaka hamidun Majeed,

Na kisha baada ya kisomo hicho basi ndio Unaomba Dua uitakayo, au kama tutakavyofahamishana zaidi hapo baadae Inshaa Allah katika Ufafanuzi zaidi.

Kwani kama tulivyoona kua kuna tofauti baina ya Tahiyyat ya kwanza na ya Mwisho ambayo ina Salat Ibrahimiyah. Hivyo kabla ya kuendelea mbele zaid basi kuna Suali ambalo baadhi yetu wanaweza wakajiuliza ambalo ni kua: '**Kwa Kua Tahiyyat Mbili hizi ni Tofauti kwani kuna Tahiyyat ya mwanzo ambayo ni fupi na kisha kuna Tahiyyat ya pili ambayo ni ndefu**, **Sasa tuseme kua Mtu ameingia Msikitini kwa Ajili ya Sala ya Rakaa Tatu ama Nne, na akakuta Jamaa imeshaanza, na Imam yuko katika Rakaa ya Tatu na yeye akaunganisha.Ambapo Kwa maana hio basi pale Imam atakapokaa kwa ajili ya Tahiyyat ya mwisho iwe katika Rakaa hio ya Tatu au ya nne.'**

'Jee Maamuma huyu aliechelewa na kukosa Tahiyyat ya kwanza ya Imam, lakini kawahi Tahiyyat ya mwisho ya Imam, ambapo kwake yeye Maamuma itakua ni Tahiyyat ya Kwanza hivyo Jee basi yeye Maamuma atatakiwa asome Tahiyyat gani?'

Naam..kupata Jawabu la Suali hili basi tunamkamata Imam alieishi kwa mda wa Umri mrefu zaidi, Imam ambae alisomesha Wanafunzi kuanzia Mababa hadi wajukuu wa Wanafunzi wake,kwani aliishi kwa mda wa Miaka 100.Huku akiwa Bingwa wa Fiqh, Usul Al Fiqh, Ilm Al Hadith, Usul Al Hadith, Tafsir, Lugha, Ilm Al Qiraa Al Qur'an, Nahw, Ilm Al Kalam, Tasawwuf, Ilm Mantiq, Tarikh, Hisabat, Ilm Nujum, Ilm Sayar n.kAkisoma yote hayo kutoka kwa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajr Al Asqallani Al Shafii,Imam Jalladin Al Mahali Al Shafii, Al Imam Alama Ad Din Al Bulqini Al Shafii, Imam Sharaf Ad Din Al Munawi Al Shafii n.k

Huyu si Imam mwengine yeyote isipokua ni Shaykh Ul Islami, Al Aalama, Qadhi Al Qudha Hamil Liwaa Madhhab Al Shafii Imam Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Ibn Muhammad Ibn Ahmad Al Ansari Al Shafii.

Maarufu kama Imam Zakkariyah Al Anasari, **Ambapo miongoni mwa Wanafunzi wake unakutana na vichwa vyenye kutisha kwa wingi wa Ilm kama vya kina Al Muhaqqiq Shaykh Ul Islami Imam Ibn Hajar Al Haytami, Shaylh Ul Islami Imam Shihab Ad Din Al Ramli, Imam Al Shaarani, Imam Al Khatib Al Shirbini, Shaykh Ul Islami Imam Shams Ad Din Al Ramli,Imam Al Qastallani, Imam Al Sakhawi, Imam Al Suyuti, Imam Nasr Ad Din Al Tablawi n.k.'**

Hivyo anasema Imam Zakarriyah Al Ansari katika kitabu chake chenye upekee cha Asna Matalib kua: '**Kama Maamuma akimuwahi Imam katika Tahiyyat ya Mwisho ambayo hua ni Tahiyyat ya Maamuma, basi Maamuma husika nae Humbidi kusoma Tahiyyat ya Mwisho katika kikao chake hicho cha Tahiyyat ya Mwanzo kwake yeye**. **Kwani hua si Makruh kwake yeye kusoma Tahiyyat ya Mwisho katika Wakati wa Tahiyyat ya Mwanzo kutokana na kua ni Mwenye kumfuata Imam.'***(Asna Matalib Fi Sharh Rawdha Talib)*

Ambapo Mtizamo huo pia ndio ulioelezewa na Wanafunzi wa Imam Zakarriyah Al Ansari kama Imam Ibn Hajar Al Haytami, Imam Shams Ad Din Al Ramli (Baba Wa Imam Shihab Ad Din Al Ramli) Imam Shihab Ad Din Al Ramli mwenyewe, Imam Ahmad Ibn Qasim Al Abadi kama ilivyoelezewa katika Hashiyat Al Sharwani.

Baada ya kuangalia kuhusiana na hilo basi mbele yetu kuna Suali jengine linalouliza kuhusiana na kutumia neno *Sayyidna* katika Salat Ibrahimiya kwa kusema:***Allahumma Ssalli aAla Sayyidna Muhammad wa Aalihi Sayyidna Muhammad Kama Sallaita aAla Sayyidna Ibrahima wa aAla Ali Sayyidna Ibrahima Innaka Hamidun Majidun.***

Allahuma Barik Aala Sayyidna Muhammad wa aAla Ali Sayyidna Muhammad Kama Barakta Sayyidna Ibrahim wa Aala Ali Sayyidna Ibrahim Innaka Hamiun Majidun

Ambapo tunatudi tena kwa Al aAlama, Al Imam Zakarriyah Al Ansari ambae anasema katika kitabu chake chenye upekee katika *Fiqh cha Asn Matalib Sharh Rawda Talib* kua: '**Imam Ibn Dhahira amesema Kua inapendekezwa zaidi kuongeza neno Sayyidna,kama ilivyoelezewa na wengi miongoni mwa Wanazuoni, na hata Jalal Al Mahali ametoa Fatwa kuhusiana nalo pendekezo hilo kwa kusema:Ndani yake kusema hivyo hua kuna kufanya jambo ambalo limeamrishwa kufanywa na ndio ukamilifu wa Adabu hasa, kwani kusema maneno hayo hua ni bora zaidi kuliko kutoyasema.'**

Na ama kuhusiana na Hadith iliyosema kua "*Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Msiniite mimi kwa jina la Sayyidna katika Sala" basi hio ni Hadith isiyokua Sahih. **Ni ya**

kutunga na isiyokua na msingi wowote kama ilovyothibitishwa na Wanazuoni wa Hadith.'*(Asna Matalib Sharh Rawda Talib)*

Ama kwa upande wa Al Muhaqqiq Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii basi nae amesema kua: '**Na Inapendekezwa zaid kutumia neno Sayydina katika Salat Ibrahimiya**h'*(Tuhfah Al Mutaj)*

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Al Ramli Al Shafii katika Nihayat Al Muhtaj na pia Imam An Nawawi katika Minhaj Talibin.

Na ingawa tumenukuu Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Jambo hili lakini hata hivyo Mtizamo huo pia ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Abu Hanifa pia. Kwanikwa upande wa Imam Muhammad Ala Din Al Haskafi al Hanafi anasema yeye katika Dar al Mukhtar kua**: ' Inapendekezwa zaidi kuongeza neno Sayyid katika Salat Ibrahimiyyah.'**

Na kwa upande wa Al Muhakkik Al Aalama Ibn Abidin Ash Shami basi nae anasema kua**: 'Haitakiwi katika Shahada pale unaposema wa Ashhad Ana Muhammadan Aabduhu wa Rasuluhu kutumia neno Sayyidna**. **Lakini inapendekezwa kutumia Sayyidna katika Salat Ibrahimiya'***(Radd Al Mukhtat - Hashiyyah Ibn Abidin)*

Imam Ibn Aabidin anaendelea kusema kua: '**Kuna baadhi waliosema kua neno Sayyidina linaweza kutumika kwa *Allah Subhanah wa Taala* tu pekee, kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu pekee ndie Sayyid.Lakini hata hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema pia kua:'Mimi ndie Sayyid wa Watoto wote wa Kizazi cha Adam.'**

'Na kuna waliosema kua Haikubaliki kusema Sayyid kua ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* na huu ni Mtizamo wa Imam Malik.Lakini ukweli ni kua bila ya shaka hua inakubalika kulitumia kwa Ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pia kwani neno Sayyid kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua linamaanisha kua Yeye ndie anaehitajika zaidi kwa Kila kiumbe, na linapotumika kwa viumbe hua linamaanisha kua Mhusika kua ni Mtukufu,Mcha Mungu na pia humaanisha Kiongozi.'*(Dar Al Mukhtar)*

Amesema Imam Abd Rahman Ibn Abi Layla kua: **'Alisema Ka'b Ibn Ujrah *Radhi Allahu Anhu* kutuambia Sisi kua:Jee Nikuzawadieni?'**

Kisha Akasema: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Alitufuata Sisi nasi tukamwambia kua: Ya Rasul Allah! Hakika Sisi Tunajua Namna ya Kukutumia Salam, lakini Jee tutawezaje sisi kukusalia?'

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema*: 'Nisalieni kwa kusema:

اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ عَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ وَ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ عَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

Allahumma Ssalli aAla Muhammad wa aAla Aalihi Muhammad Kama Sallaita aAla Ibrahima wa aAla Ali Ibrahima Innaka Hamidun Majidun.

Allahuma Barik Aala Muhammad wa aAla Ali Muhammad Kama Barakta Ibrahim wa Aala Ali Ibrahim Innaka Hamiun Majidun.(Sahih Bukhari na Muslim)

Tafsir : ***Ya Allah Muingize kwenye Fadhila na Rehma zako Muhammad (Salallahu Alayhi wa Salam) na Familia Yake kama ulivyoiingiza kwenye Fadhila na Rehma zako Ibrahim na Familia ya Ibrahim, kwani kwa hakika wewe ni Mwenye Kustahiki kusifiwa kwa sifa nzuri na Utukufu.***

Ya Allah mbariki Muhammad (Salallahu Alayhi wa Salam) Na Familia yake kama Ulivyombariki Ibrahim na Familia yake Ibrahim, kwani kwa hakika wewe kustahiki kusifiwa kwa sifa nzuri na Utukufu.

Ambapo anasema Imam Abu Bakr Ahmad Ibn Husayn Ibn Ali Ibn Musa Al Khusrawjirdi Al Bayhaqi kua: '**Imam Al Halimi amesema kuhusiana na maana ya Salat Nabii hii ni Mithili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliposema kuhusiana na Malaika waliposema katika Nyumba ya Nabii Ibrahim walipomtembelea na kumwambia Sarah kua:**

﴿قَالُوٓاْ أَتَعۡجَبِينَ مِنۡ أَمۡرِ ٱللَّهِ رَحۡمَتُ ٱللَّهِ وَبَرَكَاتُهُۥ عَلَيۡكُمۡ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِۚ إِنَّهُۥ حَمِيدٞ مَّجِيدٞ﴾

Qaloo ataAAjabeena min amri Allahi rahmatu Allahi wabarakatuhu AAalaykum ahla albayti innahu hameedun majeedun*(Surat Hud 11:73)*

Tafsir: ***Wakasema Unasataajabu juu ya majaaliwa ya Allah? Rehma za Allah Na Baraka zakeiwe Juu yenu Enyi Watu wa Nyumba hii (ya Ibrahim Khalillu Allah Kwani Kwa Hakika Allah Subhanah wa Ta'ala ni Kustahiki Sifa Nzuri zote na Utukufu.***

Naam...Imam Al Bayhaqi anaendelea kuelezea Alivyofafanua Imam Abu Abd Allah Al Halimi Al Qadhi Al Husayn Ibn Hasan Ibn Muhammad Ibn Halim Al Bukhari Al Jurjani Al Shafii kua: '**Hakika sisi tunajua kua Mtume wetu *Salallahu Alayhi wa Salam* ni mwenye kutokana na Familia ya Nabii Ibrahim Khalillu Allah,kama vile ilivyokua kwa familia yake yote. Hivyo maana ya kusema kwetu:**

اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ عَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْراهيمَ وَ عَلَى آلِ إِبْرَاهيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ وَ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَ عَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ

'Allahumma Ssalli aAla Muhammad wa aAla Aalihi Muhammad Kama Sallaita aAla Ibrahima wa aAla Ali Ibrahima Innaka Hamidun Majidun. Allahuma Barik Aala Muhammad wa aAla Ali Muhammad Kama Barakta Ibrahim wa Aala Ali Ibrahim Innaka Hamiun Majidun

Hua kunamaanisha: Ya Allah Yakubalie Maombi ya Malaika wako waliomuombea Nabii Ibrahim na Familia yake, pale waliposema:

﴿قَالُوٓاْ أَتَعۡجَبِينَ مِنۡ أَمۡرِ ٱللَّهِ رَحۡمَتُ ٱللَّهِ وَبَرَكَاتُهُۥ عَلَيۡكُمۡ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِۚ إِنَّهُۥ حَمِيدٞ مَّجِيدٞ﴾

Qaloo ataAAjabeena min amri Allahi rahmatu Allahi wabarakatuhu AAalaykum ahla albayti innahu hameedun majeedun*(Surat Hud 11:73)*

*Tafsir:**Rehma za Allah Na Baraka zakeZiwe Juu yenu Enyi Watu wa Nyumba hii (ya Ibrahim Khalillu AllahKwani Kwa Hakika Allah Subhanah wa Ta'ala ni Kustahiki Sifa Nzuri zote na Utukufu.***

Hivyo ya Allah basi na muingize Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* na Familia yake katika Rehma, Fadhila na Baraka zako, kama vile ulivyomkubalia yeye Nabii Ibrahim katika wakati wake kwani Nabii Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam* ni mwenye kutokana na Familia ya Nabii Ibrahim' *(Al Shua'b Al Iman - Imam Al Bayhaqi)*

Na mbali ya Hadith ya Ka'b Ibn Ujrah *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Salat Ibrahimiyya katika Sala, lakini pia kuna Hadith ya Abu Humayd As Saadi *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua:

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ يُوسُفَ، أَخْبَرَنَا مَالِكُ بْنُ أَنَسٍ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي بَكْرِ بْنِ مُحَمَّدِ بْنِ عَمْرِو بْنِ حَزْمٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ عَمْرِو بْنِ سُلَيْمٍ الزُّرَقِيِّ، أَخْبَرَنِي أَبُو حُمَيْدٍ السَّاعِدِيُّ ـ رضى الله عنه ـ أَنَّهُمْ قَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ كَيْفَ نُصَلِّي عَلَيْكَ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " قُولُوا اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَأَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَأَزْوَاجِهِ وَذُرِّيَّتِهِ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ".

Amesema Abd Allah Ib Yusuf kua amesema Malik Ibn Anas kua amesema Abd Allhi Ibn Abi Bakr Ibn Muhammad Ibn Umar Ibn Amr Ibn Hazm kua aamesema Baba yake kua amesema Amr Ibn Sulami Ibn Zuraqqi kua amesema Abu Humayd As Sadadi kua:

'Watu walimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kwa kusema: Ya Rasul Allah Jee Tumuombe *Allah Subhanah wa Ta'ala* vipi ili akuingize kwenye Baraka zake?

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua Semeni: '*Allahuma Salli aAla Muhammad wa Azwajihi wa Dhuriyatihi Kama Salatta aAla Ali Ibrahima, Wabarik aAla Muhammad Wa Azwajihi wa Dhuriyatihi kama Barik aAla Ibrahima Innaka Hamidun Majidun.'*

*Tafsir : **Ya Allah Muingize kwenye Fadhila na Rehma zako Muhammad (Salallahu Alayhi wa Salam) na Wake zake na Kizazi chake kama ulivyoiingiza kwenye Fadhila na Rehma zako Ibrahim na Familia ya Ibrahim.***

Ya Allah mbariki Muhammad *(Salallahu Alayhi wa Salam)* Na Wake zake na Familia yake kama Ulivyombariki Ibrahim na Familia yake Ibrahim, kwani kwa hakika wewe kustahiki kusifiwa kwa sifa nzuri na Utukufu*(Sahih Bukhari na Muslim)***

Hivyo hii ni aina ya pili miongoni mwa aina mbili za Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya mwisho ya Sala, na Wanazuoni wanasema kua inaruhusika kuchangua Moja kati ya Aina mbili hizi kama ilivyoelezwa katika Majmua Fiqhiyyah Al Quwaytiya, Rawda Talibin ya Imam An Nawawi na Fat-h Al Bar ya Imam Ibn Hajar Al Asqallani.

Ambapo anasema *Mujaddid Ad Din* Imam Shibah Ad zdin Abu Fadhl Ibm Hajar Al Asqallani kua: '**Wanazuoni wengi ni wenye Mtizamo wa kua Salat An Nabii Yeyoye inayojitosheleza katika**

kusudio la Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hua inakubalika, lakini tunapozungumzia Salat An Nabii katika Tahiyyat ya Sala basi hua inatakiwakwa Mtu anaesali kua ni mwenye kushikamana na maneno ya Salat An Nabii zilizonukuliwa katika Hadith bila ya kuondoa neno hata moja ili kuhakikisha kua ni mwenye kufuata Sunna ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ama kuhusiana na maneno yake basi ni kama tunavyoona kua ni yenye kuainisha kuhusiana na Salat An Nabii tu, bila ya kua na Salam ndani yake. Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametuamrisha sisi kua ni wenye kutakiwa kumsalia na kumtumia *Salam Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kama alivyosema katika Qu'an kua:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلاَئِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِيِّ يأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ صَلُّواْ عَلَيْهِ وَسَلِّمُواْ تَسْلِيماً﴾

Inna Allaha wamala-ikatahu yusalloona AAala alnnabiyyi ya ayyuha alladheena amanoo salloo AAalayhi wasallimoo tasleeman*(Surat Al Ahzab 33:56)*

*Tafsir:**Hakika Ya Allah na Malaika wake Wanamsalia Nabii Muhamad Salallahu Alayhi wa Salam Hivyo Enyi wale ambao Mlioamini Msalieni na Mtumieni Salam kwa Njia ya Kislam.***

Hivyo Wanazuoni wamesema kua ni Makruh kwa Mtu kua kila siku ni mwenye Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* bila ya Kumsalimia, au kumsalimia bila ya Kumsalia. Lakini kama akitumia njia zote kwa badhi ya wakati au Salat An Nabii pekee kaa baadhi ya wakati, au Salaam kwa baadhi ya wakati basi Mtu huyo hua ni mwenye kufuata Amrisho la kama ilivyosema Aya.'*(Fat-h Al Barr)*

Kwani ingawa kuna Salat An Nabii zinazojumuisha pia na kuwasalia Mitume wengine lakini tunapoiangalia Salat An Nabii ya Tahiyyat ya mwisho basi tunaona imechaguliwa Salat Ibrahimiyyah yaani yenye kumsalia na Nabii Ibrahim Alayhi Salatu wa Salaam pia.

Na hii ni kwa sababu kadhaa zilizojaa Hikma ndani yake zilizopelekea Kuchaguliwa kwa Nabii Ibrahim Khalilli Allahu kuwemo katika Salat An Nabii ya Ndani ya Sala.

Ambapo Miongoni mwao Hikma hizo ni pamoja na:

1-Nabii Ibrahim Alimuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* amjaalie kua awe ni Ulimi wa Ukweli na Haki

2-Nabii Ibrahim ndie Nabii wa Kwanza aliewaita Waislam kwa Jina la Waislam.

3-*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni mwenye kutokana na Wito wa Dua ya Nabii Ibrahim, pale aliposema:

﴿رَبَّنَا وَٱبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولاً مِّنْهُمْ يَتْلُواْ عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلْكِتَابَ وَٱلْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنتَ ٱلعَزِيزُ ٱلحَكِيمُ﴾

Rabbana waibAAath feehim rasoolan minhum yatloo AAalayhim ayatika wayuAAallimuhumu alkitaba waalhikmata wayuzakkeehim innaka anta alAAazeezu alhakeemu *(Surat Al Baqara 2:129)*

Tafsir: ***Ewe Mola wetu! Watumie (Vizazi vyetu hivyo) kutoka miongoni mwao Mtume. Ambae atawasomea aya zako na kuwaelimisha juu ya Kitabu chako na Hikma na wape Utukufu. Kwani kwa hakika wewe ni mwenye uwezo juu ya kila kitu na ni mwingi wa Hikma'***

Napia pale zilizposema tena aya:

﴿وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ ٱجْعَلْ هَٰذَا ٱلْبَلَدَ آمِناً وَٱجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعْبُدَ ٱلأَصْنَامَ۞ رَبِّ إِنَّهُنَّ أَضْلَلْنَ كَثِيراً مِّنَ ٱلنَّاسِ فَمَن تَبِعَنِي فَإِنَّهُ مِنِّي وَمَنْ عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ۞رَّبَّنَآ إِنِّيۤ أَسْكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيْرِ ذِى زَرْعٍ عِندَ بَيْتِكَ ٱلْمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُواْ ٱلصَّلاَةَ فَٱجْعَلْ أَفْئِدَةً مِّنَ ٱلنَّاسِ تَهْوِيۤ إِلَيْهِمْ وَٱرْزُقْهُمْ مِّنَ ٱلثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ۞ رَبَّنَآ إِنَّكَ تَعْلَمُ مَا نُخْفِي وَمَا نُعْلِنُ وَمَا يَخْفَىٰ عَلَى ٱللَّهِ مِن شَيْءٍ فِي ٱلأَرْضِ وَلاَ فِي ٱلسَّمَآءِ۞ ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى وَهَبَ لِي عَلَى ٱلْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ ٱلدُّعَآءِ۞ رَبِّ ٱجْعَلْنِي مُقِيمَ ٱلصَّلاَةِ وَمِن ذُرِّيَّتِي رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَآءِ۞ رَبَّنَا ٱغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَىَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ ٱلْحِسَابُ﴾

Wa-idh qala ibraheemu rabbi ijAAal hadha albalada aminan waojnubnee wabaniyya an naAAbuda Al asnama; Rabbi innahunna adhlalna kathiiran mina alnnasi faman tabiAAanee fa-innahu minnee waman AAasanee fa-innaka ghafoorun raheemun;Rabbana innee askantu min dhurriyyatee biwadin ghayri dhi zarAAin AAinda baytika almuharrami rabbana liyuqeemoo alssalata faijAAal af-idatan mina alnnasi tahwee ilayhim waurzuqhum mina alththamarati laAAallahum yashkuroona.Rabbana innaka taAAlamu ma nukhfee wama nuAAlinu wamayakhfa AAala Allahi min shay-in fee Al ardhi wala fee alssama/-I; Alhamdu lillahi alladhee wahaba lee AAala alkibari ismaAAeela wa-ishaqa inna rabbee lasameeAAu alddu AAa/-I; Rabbi ijAAalnee muqeema alssalati wamin Dhurriyyatee rabbana wtaqabbal duAAa/-I; Rabbana ighfir lee waliwalidayya walilmu/mineena yawma yaqoomu alhisabu*(Surat Ibrahim 14:35-41).*

Tafsir: ***Na (kumbuka)wakati (Ibrahim)aliposema: Ewe Mola wangu ujaalie Mji huu (wa Makkah) kua ni wenye Usalama na Amani, na nijaalie mimi na kizazi changu kua mbali na wenye kuabudu Masanamu. Ewe Mola wangu, Kwa hakika wamewapotosha watu wengi miongoni mwa Ibn Adam. Lakini yule utakaenifuata mimi, basi ni hua ni miongoni mwangu na atakaeniasi basi hakika wewe ni mwingi wa usamehemuu na mwingi wa Rehma. 'Ya Rabbi! Nimewacha kizazi changu kiishi katika bonde lisilokua na kitu, pembeni ya nyumba yako tukufu (Ka'bah), ili Ewe Mola wetu, wapate kusimamisha Sala, hivyo zijaze mapenzi nyoyo za watu miongoni mwao juu yao, na (Ya Allah) waruzuku matunda ili wapate kukushukuru; Ewe Mola wangu hakika wewe ni mwenye kujua tuliyojificha kuyafanya na tuliyoyaweka wazi. Bila ya shaka hakuna kinachofichikana kwa Allah ardhini na mbiguni; Shukrani zote anastahiki Allah ambae ndie alienipendelea mie kwa kunipa uzeeni Ismail na Is-haq. Hakika Mola wangu ni mwenye kusikia Maombi yote; Ya Rabbi nijaalie mie***

kua ni mwenye kusimamisha Sala na kizazi change pia. Mola wetu nikubalie Dua yangu. Mola wetu, Nisamehe mimi na wazazi wangu na Waislamu wote katika siku ya Malipo'.

4-Nabii Ibrahim *Alayhi Salam* baada ya Kulinyanyua Jengo la Al Kaabah basi Aliuombea Dua Ummat wa Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam kama zinavyosema aya:*

﴿وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ ٱلْقَوَاعِدَ مِنَ ٱلْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّآ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ۞ رَبَّنَا وَٱجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ عَلَيْنَآ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ۞رَبَّنَا وَٱبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولاً مِّنْهُمْ يَتْلُواْ عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلْكِتَابَ وَٱلْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَزِيزُ ٱلحَكِيمُ﴾

Wa-idh yarfaAAu ibraheemu alqawaAAida mina albayti wa-ismaAAeelu rabbana taqabbal minna innaka anta alssameeAAu alAAaleemu; Rabbana waijAAalna muslimayni laka wamin dhurriyyatina ommatan muslimatan laka waarina manasikana watub AAalayna innaka anta alttawwabu alrraheemu; Rabbana waibAAath feehim rasoolan minhum yatloo AAalayhim ayatika wayuAAallimuhumu alkitaba waalhikmata wayuzakkeehim innaka anta alAAazeezu alhakeemu *(Surat Al Baqara 2:127-129)*

Tafsir: ***Na kumbuka wakati Ibrahim alipokua akinyanyua pamoja na Ismail msingi wa Nyumba (Al Kaabah) (waliomba kwa kusema): 'Ewe Mola wetu! Tukubalie jambo letu hili. Kwani kwa hakika wewe ni mwingi wa Kusikia na ni mwenye kujua kila kitu. Ewe Mola wetu! Tujaalie sisi tuwe ni wenye kujisalimisha kwako na vizazi vyetu na Ummah wetu ujisalimishe kwako, na tuoneshe Manasika (njia au hatua zinazohitajika kufanywa katika Hija na Umra) na utukubalie toba zetu. Kwani kwa hakika wewe ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa Rehma. Ewe Mola wetu! Watumie (Vizazi vyetu hivyo) kutoka miongoni mwao Mtume. Ambae atawasomea aya zako na kuwaelimisha juu ya Kitabu chako na Hikma na wape Utukufu. Kwani kwa hakika wewe ni mwenye uwezo juu ya kila kitu na ni mwingi wa Hikma'***

5-Nabii Ibrahim *Alayhi Salatu wa Salam* ndie Nabii pekee ambae alimpa *Salam Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kuusalimia Umati wa *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam*Katika Usiku wa Safari ya Miraj walipokutana Mbinguni

6-Tunapomsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hua tunamuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* ampandishe Darja zaidi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ya kua na Urafiki nae kama alivyokua na Urafiki na Nabii Ibrahim *Alayhi Salatu wa Salaam.*

Na hii hua kamwe haimshushi Darja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Kutokana na kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndie Kiumbe bora aliewahi Kuumbwa Na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Bali hua inamanisha kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliempendekeza kwa kumuingiza katika Rehma na Baraka Nabii Ibrahim na Familia yake basi na Amfanyie hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Familia yake pia.

Na hii pia ni Kutokana na kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Kuomba kwake yeye mwenyewe na kuuombea Ummah wake, na familia yake na kila atakaemfuata kupata heshima hio ya kuombewa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwani Maombi hua hayapatikani kabla ya kuombwa kwani kinachoombwa huombwa katika wakati ambao anaeomba hua hana kitu hicho anachokihitajia.

Kwani katika Siku ya Malipo wakati Mitume wote wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* watakua wakisema 'Nafsi yangu Nafsi yangu'Basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* atapewa Nafsi ya Kuomba Dua ambayo atajibiwa, ambapo nae atauombea Ummah wake kwa kusema Ummah Wangu, Ummah Wangu. **Na Maombi yake hayo yatakubaliwa ya Kuuombea Ummah wake*(****Sahih Bukhari)***

Anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaambia Masahaba zake *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Miongoni mwa Watu watakaopendwa sana nami katika Ummah wangu watakua ni wale watakaokuja baada yangu, kwani kila mmoja angetamani kuniona japo kidogo thamani ya Familia yake na Mali yake.'***(Sahih Muslim)*

Hivyo katika kumsalia kwetu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hua ni wenye kupandisha Darja yeye na utajo wake hapa Duniani na hivyo hua ni wenye kusaidia katika kuipeleka mbele Dini ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuipa ushindi dhidi ya maadui zake, na hua ni kusimamia amrisho la *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Sharia zake.

Ama kwa upande wa Kiahera basi hua ni wenye kupata Malipo makubwa sana, na kudhihirisha kukubaliana nae katika kushikamana na Ummati wake na pia kumuombea kupata darja ya kupanda katika Darja ya Maqamam Mahmuda.

Na Miongoni mwa Manufaa ya Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika *Salat Ibrahimiyyah* ndani ya Sala hua ni Kupata Uombezi wake, na kuonesha Mapenzi yetu juu yake *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Pia hua ni kufanya Ibada kwa kutekeleza amrisho la *Allah Subhanah wa Ta'ala* la *Kumsalia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hua ni kuenda Sambamba katika Kupata Malipo na Malaika wenye kufanya Ibada hio ya Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hua ni kupandishwa Darja mara 10 kwa kila Salat Moja.

Hua ni Kulipwa Thawabu 10 na kufutiwa Dhambi 10.

Hua ni Kupewa Baraka mara 10.

Hua ni Kukubaliwa kwa Sala na Dua zilizomo ndani yake.

Hua ni kuongezea Riziki kwa kuonesha Shukran kutokana na *Kumsalia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hua ni Kutafutakua na Ukaribu na *Rasul Allah Salallahu alayhi wa Salam* katika Siku ya Malipo.

Hua ni sawa na Kutoa Sadaka ndani ya Ibada ya Sala yako.

Hua ni Kusaliwa na kuombewa Na Malaika kwa Anaemsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hua ni kuupata Utulivu katika Siku ambayo Nyoyo za Watu zitakua zimejaa Khofu.

Hua ni chanzo cha Nuru katika Kuvuka Daraja la Sirat.

Hua ni Kuulainisha Moyo na kutoufanya kua Mgumu.

Hua ni Kuingizwa ndani ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kumuombea Rehma Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kua ni mwenye kuwasilishwa Jina lako mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutokana na Kumsalia kwako.

Hua ni kumtekelezea Haki yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, n.k.

Hivyo Sala ina faida nyingi sana na manufaa makubwa sana kwetu, kwani hizo ni baadhi tu ya faida za Salat Nabii wacha mbali Dhikr ufanyazo ndani yake, Aya usomazo ndani yake, Dua n.k. Hivyo hua haishangazi kuona kua Dhambi hua zinapukutika kwa kila wakati unapokua ndani ya Ibada ya Sala.

Na amesema Imam Salim bin Sumair Al Hadrami, kua

تَشدِيدَاتُ التَّشَهُّدِ إحدَى وَعِشْرُونَ: خَمْسٌ فِي أَكْمَلِهِ وَسِتَّةَ عَشَرَ فِي أَقَلِّه:

ا(التَّحيَّاتُ) عَلَى التَّاءِ وَاليَاءِ (المبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ) عَلَى الصَّاد، (الطَّيِّباتُ) عَلَى الطَاءِ وَاليَاء، (لله) عَلَى لَامِ الجَلَالَةِ، (السَّلامُ) عَلَى السِّينِ، (عَلَيكَ أيُّها النَّبيّ) عَلَى اليَاءِ والنُّونِ وَاليَاءِ، (ورَحمَةُ اللهِ) عَلَى لَامِ الجَلَالةِ، (وَبرَكَاتُهُ السَّلامُ) عَلَى السِّينِ، (عَلَينَا وَعَلَى عِبَادِ اللهِ) عَلَى لَامِ الجَلَالَةِ، (الصَّالِحِينَ) عَلَى الصَّادِ، (أشهَدُ أن لَّا إلَه) عَلَى لَامِ أَلِفٍ، (إلَّا الله) عَلَى لَامِ أَلِفٍ وَلَامِ الجَلَالَةِ، (وأَشْهَدُ أنَّ) عَلَى النُّونِ، (مُحَمَّدًا رَسُولُ اللهِ) عَلَى مِيمِ مُحَمَّدٍ وَعَلَى الرَّاءِ وَعَلَى لَامِ الجَلَالةِ

Tahiyyat ina Tashaddad 21 ambapo 5 miongoni mwao ni pale ikisomwa kwa ukamilifu na 16 kama ikisomwa kwa kifupi ambazo ni:

- **Tashshadid katika huruf‘ta’ na ‘ya’** التَّحِيَّاتُ
- **Tashshadid katika huruf ‘sad’** المُبَارَكَاتُ الصَّلَوَاتُ
- **Tashshadid katika huruf ‘ta’ na ‘ya’** الطَّيِّبَاتُ
- **Tashshadid katika huruf ‘lam Al Jalalah’** لِلَّهِ

- **Tashshadid katika huruf ‘sin’** السَّلَامُ
- **Tashshadid katika huruf ‘ya’, ‘nun’ na ‘ya’**عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ
- **Tashshadid katika huruf ‘lam Al Jalalah’** وَرَحْمَةُ اللَّهِ
- **Tashshadid katika huruf ‘sin’**وَبَرَكَاتهُ السَّلَامُ
- **Tashshadid katika huruf ‘lam Al Jalalah’** عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ
- **Tashshadid katika huruf ‘sad’**الصَّالِحِيْنَ
- **Tashshadid katika huruf ‘lam alif’**أَشْهَدُ أنْ لَاَّ إلَهَ
- **Tashshadid katika huruf ‘lam alif’ na ‘lam Al Jalalah’**إلَّا الله
- **Tashshadid katika huruf ‘nun’**وَأَشهَدُ أَنَّ
- **Tashshadid katika huruf ‘mim’**مُحَمَّداً
- **Tashshadid katika huruf ‘ra’ na ‘lam Al Jalalah’**مُحَمَّداً رَسُولُ اللهِ **(*Lihat Al Mujtaba fi Sharh Safinah Al Naja*)**

DUA KATIKA KIKAO CHA TAHIYYAT YA MWISHO.

❖❖❖❖

Amesema Abd Allah Ibn Amr *Radhi Allahu Anhu* kua:

عَنْ أَبِي بَكْرٍ اَلصِّدِّيقِ – رضى الله عنه – { أَنَّهُ قَالَ لِرَسُولِ اَللَّهِ – صلى الله عليه وسلم –عَلِّمْنِي دُعَاءً أَدْعُو بِهِ فِي صَلَاتِي . قَالَ قُلْ : " اَللَّهُمَّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي ظُلْمًا كَثِيرًا , وَلَا يَغْفِرُ اَلذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ , فَاغْفِرْ لِي مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ , وَارْحَمْنِي , إِنَّكَ أَنْتَ اَلْغَفُورُ اَلرَّحِيمُ } مُتَّفَقٌ عَلَيْهِ

Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu*alimwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kwa kusema: Ya Rasul Allah nifundishe Dua ambayo nitaisoma mimi ndani ya Sala zangu.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Sema:*Allahuma innee zhalamtu nafsee zhulman kabeera wa la yaghfir adh-dhunuba illa anta fagh-fir lee maghfiratan min `indika w 'arhamnee innaka anta Al ghafooru ' r-raheem

*Tafsir:***Ya Allah Hakika Mimi nimejidhulumu Nafsi yangu kwa Dhulma Kubwa sana()ya kushindwa kutekeleza majumu yangu ipasavyo juu yako) Na Hakuna Mwenye Kusamehe Dhambi isipokua wewe Hivyo naomba NisamehePate Usamehevu wakoNa Niingize kwnye Rehma zako Kwani kwa hakika wewe ni Mwingi wa Usamehevu na ni mwingi wa Rehma.(***Muttafaq aALayhi)***

Naam hivyo kwanza Tufahamiane kua hii ni Hadith yenye Sifa ya *Muttafaqun Alayhi*.Ambapo maneno Muttafaqun Alayhi kwa upande wa Ilm al Hadith basi hua yanamaanisha kua Hadith husika ni Hadith

iliyonukuliwa na Maimam wawili wakuu wa Hadith ambao ni Bukhari na Muslim na kutokana na kua na Usahihi wa hali ya juu kabisa na kuaminika sana kwa usahihi wake miongoni mwa Wanazuoni wa Hadith.

Na hadith yenye sifa ya *Muttafaq Alayhi* hua ni yenye kua na Sifa 2, kwanza Hua ni Hadith moja yenye Maneno yanayofana, au yanayo tofautiana ila maana yake hua ni maana moja bila ya kua na Utata ndani yake.

Na pili hua ni Hadith ambayo lazima Mtu wa kwanza kuinukuu awe huyo huyo mmoja, yaani awe ni Sahaba mmoja kwa mfano katika Hadith hii tunaona Sahaba aliehusika ni Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu*.

Na pia kuna Wanaosema kua *Muttafaq Alayhi* hua ni Hadith Sahih iliyonukuliwa na Imam Bukhari, Imam Muslim na Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Hivyo hio ni sifa ya kwanza ya Hadith hii kua Wamekubaliana Maimam kua ni Hadith Sahih.Kwani Hadith hii ni Hadith yenye Dua nzuri sana ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* hakumfundisha Mtu yeyote isipokua Rafiki yake kipenzi, ambae ni Al Sadiq Abu Quhafa Abu Baqr *Radhi Allahu Anhu.*

Na uzuri wake Dua iliyomo ndani yake ni kua Mtu anaeiomba Dua iliyomo ndani yake hua kwanza ni Mwenye Kukubali Udhaifu wake wa Kimaumbile Kama walivyokua Viumbe wote mbele ya Muumba wao.Na hivyo hii hua ni moja kati ya njia bora za Kuomba Dua kwa unyenyekevu ili kupata Usamehevu na kuingizwa ndani ya Rehma za *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anamwambia Sahaba wake kua Mwambie Mola wako kua kwa Hakika wewe Unajijua kua Umeifanyia Dhulma kubwa Nafsi yako kutokana na kushindwa kutekeleza Majukumu yako Ipasavyo yanayohusiana na haki za Mola wako mbali Ya kujitajid kwako kote.

Kwani Hakuna Kiumbe asiekua na kasoro katika utekelezaji wa haki za Mola wake juu yake.Na hivyo Mtu anaposhindwa kutekeleza Ipasavyo majukumu yake na kusimamia ipasavyo haki za Mola wake juu yake basi Mtu husika hua si mwenye kumkosea yeyote yule mwengine isipokua hua ni mwenye kuikosea Nafsi yake na hivyo hua ni mwenye kujidhulumu yeye mwenyewe.

Ambapo inabidi tuulizane Hivi Jee Mtu anapokua anajifisidi au anajidhulumu au Anajifilisi yeye mwenyewe n.k hua ni Mtu mwema au ni Mbaya kwa Nafsi yake?

Bila ya shaka hua ni Mbaya kwa Nafsi yake kwani amejidhulumu mwenyewe na hana wa kumlaumu.Fikiria kua Kama Malaika tu ambao hawana Khiari wala Matamanio, tangu wameumbwa hawajamuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hawatomuasi, lakini katika siku ya Malipo watalia kwa kusema Ya Allah! Tunaomba utusamehe kwani Hakika sisi hatukusimamia haki zako wewe Ipasavyo.

Naam..hivyo Kama Malaika tangu waumbwe wamekaa katika Hali ya kusujudu tu na kusema *Subhanah Rabbi Al Aala wabihamdihi* kwa miaka yote, watasema kua wamejidhulumu kwani hawakutekeleza haki za Mola wao ipasavyo. Jee mimi na wewe wenye makontena kwa Makontena ya Dhambi tutasemaje? Hatukujidhulumu nafsi zetu?

Hivyo bila ya shaka, Mimi nawe ni wenye Kujidhulumu sana Nafsi zetu, na hakuna mwenye kusamehe makosa ya Nafsi zetu ispokua Mola wetu kutokana na Ukubwa wa uwezo wake juu ya kila kitu na Uadilifu wake na Rehma na Huruma zake.

Na miongoni mwa Hadith kuna ile Hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allau Anhu* ambae amesema kua:

عن رَسولِ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ، أنَّهُ كانَ إذَا قَامَ إلى الصَّلَاةِ، قالَ: وَجَّهْتُ وَجْهي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ حَنِيفًا، وَما أَنَا مِنَ المشْرِكِينَ، إنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي، وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ العَالَمِينَ، لا شَرِيكَ له، وَبِذلكَ أُمِرْتُ وَأَنَا مِنَ المسْلِمِينَ، اللَّهُمَّ أَنْتَ المِلِكُ لا إلَهَ إلَّا أَنْتَ، أَنْتَ رَبِّي وَأَنَا عَبْدُكَ، ظَلَمْتُ نَفْسِي، وَاعْتَرَفْتُ بذَنْبِي، فَاغْفِرْ لي ذُنُوبِي جَمِيعًا، إنَّه لا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إلَّا أَنْتَ، وَاهْدِنِي لأَحْسَنِ الأَخْلَاقِ، لا يَهْدِي لأَحْسَنِهَا إلَّا أَنْتَ، وَاصْرِفْ عَنِّي سَيِّئَهَا، لا يَصْرِفُ عَنِّي سَيِّئَهَا إلَّا أَنْتَ، لَبَّيْكَ وَسَعْدَيْكَ، وَالخَيْرُ كُلُّهُ في يَدَيْكَ، وَالشَّرُّ ليسَ إلَيْكَ، أَنَا بكَ وإلَيْكَ، تَبَارَكْتَ وَتَعَالَيْتَ، أَسْتَغْفِرُكَ وَأَتُوبُ إلَيْكَ. وإذَا رَكَعَ قالَ: اللَّهُمَّ لكَ رَكَعْتُ، وَبِكَ آمَنْتُ، وَلَكَ أَسْلَمْتُ، خَشَعَ لكَ سَمْعِي وَبَصَرِي، وَمُخِّي، وَعَظْمِي وَعَصَبِي. وإذَا رَفَعَ قالَ: اللَّهُمَّ رَبَّنَا لكَ الحَمْدُ مِلْءَ السَّمَوَاتِ وَمِلْءَ الأَرْضِ، وَمِلْءَ ما بيْنَهُمَا وَمِلْءَ ما شِئْتَ مِن شَيءٍ بَعْدُ. وإذَا سَجَدَ قالَ: اللَّهُمَّ لكَ سَجَدْتُ، وَبِكَ آمَنْتُ، وَلَكَ أَسْلَمْتُ، سَجَدَ وَجْهِي لِلَّذِي خَلَقَهُ، وَصَوَّرَهُ، وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ، تَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الخَالِقِينَ. ثُمَّ يَكونُ مِن آخِرِ ما يقولُ بيْنَ التَّشَهُّدِ وَالتَّسْلِيمِ: اللَّهُمَّ اغْفِرْ لي ما قَدَّمْتُ وَما أَخَّرْتُ، وَما أَسْرَرْتُ وَما أَعْلَنْتُ، وَما أَسْرَفْتُ، وَما أَنْتَ أَعْلَمُ به مِنِّي، أَنْتَ المقَدِّمُ وَأَنْتَ المؤَخِّرُ، لا إلَهَ إلَّا أَنْتَ.

Alikua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*anaposimamakusali hua ni mwenye kusema: Allahu Ndie Mkubwa zaidi, Shukran zote zinastahiki kwa Allah Na Utukufu ni wa kwake Asubuhi na Jioni. Kwa Hakika Mimi nnauelekezea Uso wangu kwa Allah, ambae ndie alieumba Mbingu na Ardhi ambavyo vyote ni vyenye utiifu na kujisalimisha juu yake. Na mimi si miongoni mwa wale wanaomshirikisha nae *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kwani Kwa Hakika Sala zangu, Ibada zangu, Maisha yangu, Mauti Yangu ni kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala tu. Ambae ni Mola wa Ulimwengu wote asiekua na Mshirika, Na hivyo ndivyo nilivyoamrishwa kufanya, na Mimi ni Miongoni mwa Waislam (waliojisalimisha kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala*).

Wewe ni Mola wangu Mlezi, na mimi ni mja wako, nimejidhulumu nafsi yangu na nimekiri dhambi zangu, hivyo basi nisamehe madhambi yangu yote, kwani hakuna mwenye kusamehe Dhambi isipokua wewe, Niongoze kwenye maadili mema kwani hakuna mwenye kuongoza kwenye maadili mema ila wewe na niepushe naMabaya yote, Niko kwa ajili yako na kwa Matakwa yako, na kila wema wote uko mikononi Mwako, na ubaya hauko juu yako wala Kwako, Baraka zote ni kutoka kwako na Utukufu ni wako, Naomba msamaha wako na nnatubu mbele yako.

Na anaporukuu husema: Ewe Mola wangu, napiga magoti Kwako, na kwako nimekuamini, na Kwako nanyenyekea katika kusikia kwangu na kuona kwangu, na Ubongo wangu, na mifupa yangu na mishipa yangu vyote vinakunyenyekea wewe.

Na anapoinuka husema: Ewe Mola Mlezi wetu, sifa njema zoet zinastahiki juu yako, unayejaza Mbingu, na unaijaza Ardhi, na unajaza vilivyo baina yake, na unajaza Utakalo baada ya hayo.

Na anaposujudu husema: Ewe Mola wangu, mimi nakusujudia, na kwako nimekuamini, na Uso wangu nimeunyenyekesha kwa aliyeuumba, kuuependezesha na akajaalia kusikia kwake na kuona kwake,Uukufu ni wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* pekee ambae ndie mbora wa kuumba.

Kishakitu cha mwisho alichokua akisema baina ya Tashahud na Taslim ilikua ni Dua Ifuatayo: Ya Allah Nisamehe Niliyotanguliza (katika Dhambi)Na Yatakayofuata (katika Dhambi)Na Katika yaliyosiri(katika Dhambi)Na Yaliyo Dhahiri(katika Dhambi) na Katika Niliyofanya IsrafuKwani Wewe ni Mwenye kuyajua zaidi yangu Hakika wewe ni mwenye Kua Kabla ya kila kituNa wewe ndie Mwenye Kukitangulia Kila kitu Hakuna Mola isipokua Wewe(*Sahih Muslim)*

Ambapo tunapoiangalia hadithi hii ambayo ndani yake imejaa Dua ikiwemo Dua tunazozizungumzia katika sehemu hii ambayo ni Dua baada ya Tashahud ndani ya Tahiyyat kabla ya kutoa Salamu.Basi tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Msamaha kwa Madhambi yaliyotangulia, na yatakayokuja baadae ndani ya Maisha yake.

Na ingawa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameshasamehewa hayo katika Ubashirio la Ufunguzi wa Mji wa Makkah baada ya Makubaliano ya *Hudaybiyah* mnamo mwaka wa 6 Al Hijra kama ilivyosemwa katika Qur'an katika Surat Al Fatih pale ziliposema Aya:Baada ya Bismi Allahi Rahmani Rahiim:

﴿بِسْمِ اللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۞ إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحاً مُّبِيناً۞ لِّيَغْفِرَ لَكَ ٱللَّهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطاً مُّسْتَقِيماً﴾

Inna Fatahna Laka Fat-han Mubiina Liyaghfira Allahu Ma Taqaddama min Dhanbika Wama Taakhara Wayuutimma Niiamatahu Aalayka Wayahdiyyaka Sirata Al Mustaqiima *(Surat Al Fatih 48:1-2)*

Tafsir: ***Kwa Hakika Tumekufungulia wewe (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Ufunguzi (Wenye Ushindi) Mkubwa Sana UliowaziKua Amekusamehe Allah yaliyotangulia katika Dhambi zakoNa YatakayokujaNa Amekutimizia Neema zake Juu yakoNa Amekuongoza katika Njia iliyonyooka.***

Naam..hivyo mbali ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua ameshamehewa Dhambi zote lakini alijua akiiomba Dua hii ndani ya Sala yake.

Ambapo hii pia ni kwa sababu ya kutufunza sisi mimi na wewe kua tuwe ni wenye kuisoma Dua hii kwani Kimaumbile Ibn Adam hua hakosi kua na Madhambi kutokana na Udhaifu wake kinafsi.Kisha baada ya kuomba msamaha kutokana na yaliyokua na yatakayokua kulingana na utofauti wa Nyakati basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Msamaha kuhusiana na Makosa ya Siri na ya Dhahiri.

Yaani kutokana na Makosa ambayo Mtu anaweza kufanya akiwa peke yake, bila kujua au kwa kudhania Mabaya ndani ya Moyo na Ufahamu wake kwa wengine, ambapo haya yote hua ni ya Siri kwake lakini hua ni dhahiri kwa Mola wake.

Na pia kuna Makosa ya Dhahiri ambayo ni ya Kudhihirika ndani ya Ufahamu wa Mtu kua hili nililofanya ni kosa na pia Dhahiri mbele za Watu hadharani.Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaomba Msamaha kwa Mola wake kwa Kufanya Israfu.Ambapo tunapozungumzia kuhusiana na makosa ya Israfu basi haya ndio yapo mengi sana, kwani hua ni Dhambi za Kutumia vibaya, au kwa fujo au kiuzembe neema za *Allah Subhanah wa Ta'ala* alizotujaalia ambazo ndani yake.

Neema hizo kuna Neema ya Uhai, Afya, Mali,Ufahamu, Akili, Nguvu, Mamlaka, Cheo, ambazo zote hizi ukitumia, kiharamu, kiuzembe au kwa fujo basi hua ni kufanya Israfu n.k

Kuna Israfu za Neema za Viungo vya Miili yetu, kama Macho ukiangalia ya Haramu hua ni Israfu na Hii ndio Israfu kubwa zaidi katika Jamii yetu kwani leo kila unapotupa jicho basi tayari ishakua kosa unakoga dhambi za Kumwaga.Hio ni Israfu ya Macho tu, lakini kuna za Ulimi, Masikio n.k

Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kuomba kwake Msamaha basi anatufundisha kumuachia *Allah Subhanah wa Ta'ala* mwenyewe juu ya makosa na kasoro zetu kwani yeye ndie mwenye kujua zaidi juu ya kila kitu chetu kwani cha Siri na dhahiri tukijuacho na tusichokijua kua vyote hivyo Tuombe msamaha juu yake.

Na kumalizia Dua hio ya msahama kwa kuthibitisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndio wa mwanzo na wa mwisho, ndio kabla ya kila kitu na baada yakila kitu, hivyo humtanguliza amtakae na humchelewesha amtakae humzuia amtakae na kumwachia amtakae, humpandisha Darja amtakae na kumshusha amtakae, humtajirisha amtakae na kumfakirisha amtakae n.k

Na yote haya ni kutokana na Hikma zake na mapenzi yake juu ya viumbe wake kulingana na Maumbile yao kwani yeye ndie mwenye kujua zaidi ni kipi chenye kheri kwa yupi na kwa wakati gani na kwanini. Kwani Hakuna Mola isipokua yeye.

Na amesema Shaddad Ibn Aws *Radhi Allahu Anhu*kama isemavyo hadith ifuatayo kua:

وَعَن شَدَّادِ بْنِ أَوْسٍ قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ فِي صَلَاتِهِ:
اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الثَّبَاتَ فِي الْأَمْرِ، وَالْعَزِيمَةَ عَلَى الرُّشْدِ، وَأَسْأَلُكَ مُوجِبَاتِ رَحْمَتِكَ، وَعَزَائِمَ مَغْفِرَتِكَ، وَأَسْأَلُكَ شُكْرَ نِعْمَتِكَ، وَحُسْنَ عِبَادَتِكَ، وَأَسْأَلُكَ قَلْباً سَلِيماً، وَلِسَاناً صَادِقاً، وَأَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ مَا تَعْلَمُ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا تَعْلَمُ، وَأَسْتَغْفِرُكَ لِمَا تَعْلَمُ، إِنَّكَ أَنْتَ عَلاَّمُ الْغُيُوبِ)

Na amesema Shaddad Ibn Aws *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiomba Dua ndani ya Sala yake kwa kusema:

Allahuma innee as'aluka 'l-thabbaat fi 'l-amri wa'l-`azeemata `ala 'r-rushdi wa as'aluka shukra ni`amatika wa husna `ibadatika wa as'alauka qalban saleeman wa lisaanan saadiqan wa as'aluka min khayri maa t`alamu wa a`udhu bika min sharri maa ta`alamu wa astaghfiruka lima ta`lamu Innaka Anta Aalimu Al Ghuyubi.

*Tafsir:***Ya Allah hakika mimi nnakuomba Nguvu katika Kila Jambo la Kidini na Uwezo wenye Azma katika Uongofu Na Nakuomba Unijaalie Shukrani kwa Neema zakoNa Ubora katika Kukuabudu Na Nakuomba Moyo wenye IkhlasiNa Ulimi wenye Kusema Ukweli na Nakuomba**

Kheri katika kila Kitu ukijuacho **Na Nakuomba uniepushe na Shari katika Kila kituunachokijua na Nakuomba Unisamehe katika kila Jambo unalolijua, Kwani kwa h akika wewe ni mwenye kujua yasiyojulikana.***(Imam Ahmad, Imam AtTirmidhi)*

Miongoni mwa Hadith zinazoelezea kuhusiana na Dua alizokua akiomba *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* baada ya Tahiyyat ya mwisho kabla ya kutoa Salam, ni ile hadith iliyomo katika Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal na Sunnah Abu Daud ambayo inasema:

Amesema Hanzalah Ibn Ali kua amesema Muhjan Ibn Adra *Radhi Allahu Anhu* kua:

دخل رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم المسجِدَ فإذا هو برجُلٍ قد قضى صلاتَه وهو يتشهَّدُ وهو يقولُ: اللَّهُمَّ إني أسألُك يا اللهُ الأحَدُ الصَّمَدُ الذي لم يلِدْ ولم يولَدْ ولم يكُنْ له كفُوًا أحدٌ أن تغفِرَ لي ذُنوبي؛ إنَّك أنت الغفورُ الرَّحيمُ. قال: فقال: قد غُفِرَ له، قد غُفِرَ له، ثلاثًا

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliingia Msikitini akamkuta Mtu ambar anamalizia kusali Sala yake, ambapo ndani yake Mtu huyo Akatoa Shahada na kisha akaomba Dua ifuatayo:**
***Allahuma Inni As-aluka* - Ya Allah hakika Mimi nakuomba.**
***Ya Allahu Al Ahadu Al Samadu* - Ewe Allah, Mwenye Umoja Mwenye Upekee.**
***Alladhii Lam Yalid wa Lam Yulad* - Wewe Ndie Ambae Hukuzaa wala Hukuzaliwa.**
***Wa Lam Yakun Lahu Kufuwan Ahad* - Na Wala Hakuna anaefanana nawe hata mmoja.**
***An Taghfirli Dhunubi* - Kua Unisamehe Dhambi zangu.**
***Innaka Anta Al Ghafuru Al Rahiim* - Kwani wewe Ni Mwingi wa Kusamehe na Ni Mwingi wa Huruma.**
Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema mara tatu kuhusiana na Maneno ya Dua aliyoyasema Mtu huyo baada ya Tahiyyat yake hio kua:Hakika amesameheqa Dhambi zake, Hakika Amesamehewa Dhambi zake, Hakika Amesamehewa Dhambi zake.'*(Sunan Abu Daud, Sunan An Nasai, Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal)*

Kwani Hadith hii inatuonesha kua mwenye kuomba Dua hii katika Mfumo huu hakua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, na wala Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakufundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kua waombe katika Njia hio au kwa Mfumo huo.

Lakini Hata Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikubaliana na Usahih, Uzuri na Nguvu ya Dua hii iliyoombwa na Sahaba yake huyo *Radhi Allahu Anhu.* Hivyo kabla ya kuendelea kufafanua basi Hapa tunakubaliana kua Dua hii ilikua ni Bidaa iliyoanzishwa na Sahab huyu *Radhi Allahu Anhu.*

Na kwa kua ni Bidaa nzuri basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kaisifu na kuipitisha mara tatu kua Dua hio imekubaliwa.

Pili ni kua Ndani yake Dua tunaona kua imebeba Maneno Matukufu yanayomtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupitia katika Sifa zake zenye Utukufu wa kipekee katika kuthibitisha Tawhid na Ikhlasi. Kwani ni maneno ya Aya za Surat Al Ikhlasi ambayo ndani yake inafafanua Utukufu wenye Ukamilifu wa Kipekee usiokua na Mfano wake wala Mithli yake.Kwani Utukufu wa Umoja wake unajumuisha Ukamilifu katika Kila kitu chake, Sifa zake, Ukubwa wake, Majina yake, Vitendo vyake, Uwezo wake, Kujua kwake, Kusikia kwake Kuona kwake n.k.

Kwani ni maneno ya Aya za Surat Al Ikhlasi ambayo ndani yake inafafanua Utukufu wenye Ukamilifu wa Kipekee usiokua na Mfano wake wala Mithli yake.

Kwani Utukufu wa Umoja wake unajumuisha Ukamilifu katika Kila kitu chake, Sifa zake, Ukubwa wake, Majina yake, Vitendo vyake, Uwezo wake, Kujua kwake, Kusikia kwake Kuona kwake n.k. Na hivyo Utukufu wa Ukamilifu wake hauhitaji Mwenza, wala Msaidizi, wala Mzazi wala Mtoto wala yeyote wala chochote. Na hivyo Hakuzaa wala hakuzaliwa na wala Hafanani na yeyote wala na chochote.

Na ukweli ni kua Ukiiangalia utangulizi wa Dua utaona kua ni Fupi sana, lakini ina ujumbe mkubwa sana ambao uzito wake ni sawa na Robo ya Qur'an. Na hivyo Uzito huo ndio uliopelekea kukubaliwa kwa Maombi yaliyofuatia baada yake ambayo ni Kuomba Msamaha kutoka kwa Allah Subhanah wa Ta'ala aliesifiwa kwa sifa hizo za Ukamilifu wa kipekee na kisha Sahaba huyo Radhi Allahu Anhu akaifunga Dua hio kwa Kumtukuza tena *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Kuthibitisha sifa za Mwenye Kuhitajiwa Usamehevu wake ambae ni Mwingi wa Usamehevu na Mwingi wa Huruma.

Kwani anasema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu kua*: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alikua akitufundisha sisi Maneno, kwa namna ambayo si kama alivyokua akitufundisha ssi Tashahhud kwa kusema:**

وكان يُعلِّمُنا كلماتٍ ولم يكن يُعلِّمناهنَّ كما يُعلِّمُنا التشهدَ اللهمَّ ألِّفْ بين قلوبِنا وأصلحْ ذاتَ بينِنا واهدِنا سُبُلَ السلامِ ونجِنا من الظُّلماتِ إلى النُّورِ وجنِّبْنا الفواحشَ ما ظهرَ منها وما بطنَ وبارِكْ لنا في أسماعِنا وأبصارِنا وقلوبِنا وأزواجِنا وذرياتِنا وتبْ علينا إنك أنت التَّوابُ الرحيمُ واجعلْنا شاكرِينَ لنعمتِك مُثْنينَ بها قابلِيها وأَتمَّها علينا

Allahuma Alif Bayna Quluubihina **- Ya Allah Unganisha Baina ya Nyoyo zetu.**
Wa Aslih Dhaati Baynina Wahdina **- Na Suluhisha Tofauti zetu Baina yetu.**
Waahdiina Subulan Alsalini **- Na tuongoze Katika Njia yenye Usalama.**
Wanajjinnaa Mina Dhulumati wa Nur **- Na Tuokoe kutoka katika Kiza tuingize kwenye Nuru.**
Wajjanibnaa Al Fawahisha ma Dhahara minha wama Battan **- Na Tuepushe na Madhambiya Matamanio yakiyodhahiri na Yaliyofichikana.**
Wabariklana Fii Asmaa'ina, wabsariina Waqlubiina **- Na Tuungezee baraka katika kusikiliza kwetu na Kuangalia kwetu na kutafakkari Ndani ya Nyoyo zetu.**
Wa Azwajina wa Dhurriyatina **- Na Kwa Wenza wetu (Wake zetu/Waume zetu) na Vizazi vyetu.**
Wa Tub Alayna Innaka Anta Tawwabu Al Rahiim **-Na Tusamehe kwani kwa Hakika wewe ni Mwenye Kusamehe na Mwenye wingi wa Huruma.**
Wa Jaalna Shakiran Liniamaatika **- Na Tujaalie kua na Shukran kwa Neema zako.**
Muthnayna biiha Qabliha Waatam Aalayna **- Tuzitukuze, Tuzikubali kwa Kututimizia kwako.'***(Imam Ibn Hibban, Imam At Tabrani, Imam Al Hakim)*

Subhanah Allah!
Hadith inatuonesha aina ya Dua Nzuri sana ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* alikua akuwafundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kwa ajili ya Kuzisoma katika Sala baada ya Tahiyyat na Kabla ya Kutoa Salam ya kumaliza Sala.

Na tunapoangalia mifano ya Dua hizi basi ndio tunaona wazi ni kwanini Wanazuoni wakasema kua: **‘Inakubalika kuomba Dua yoyote aitakayo Mtu kuhusiana na mambo ya Kihalali ya Kidunia na ya Kiakhera. Lakini hata hivyo hua inapendekezwa zaidi kusoma Dua ambazo zinapatikana kwenye Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.’***

Ambapo tunapoangalia Mfano wa Dua hii akiyofundishwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* na Masahaba wengineo basi tunaona kua: ‘**Mbali ya kua Dua hii ilifundishwa katika Nyakati hizo lakini pia imekua kama kwamba *Rasul Allah Salallah Aalayhi wa Salam* anatuona hali tuliyokua nayo leo hii sisi Waislam.Na hivyo kua ni mwenye kutuachia Dawa pekee ya kutatulia Matatizo na Mashakil yetu mengi sana yaliyotuzonga leo hii katika Ummah wake huu na hivyo kupitia katika Maombi ya Dua hii basi Mashakil yote yatatoweka.’**

Kwani Duaa iko wazi, na hivyo kutudhihirishia Miujiza ya Utume wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika wakati wa Uhai wake na baada ya kufariki kwake na baada ya muda mrefu wa kutokuwepo kwake hadi katika Wakati wetu na utakaofuata.

Na hakuna atakaekataa kua Kisomo cha Maombi ya Dua hii ndio Kisomo cha Maombi ambacho tunakihitajia Sana katika Wakati wetu.Kwa ajili ya Kuomba Umoja wetu Waislam ambao leo hatuna, na hivyo Wapalestina Wanadhulumiwa na kuangamizwa na Wazayuni lakini sisi tumekaa tunangalia tu hii ni kwa sababu ya kukosekana kwa Umoja wa Waislam, na hivyo tunadharuliana, na kubaguana.

Hivyo kuna hitajio la Kuomba Dua hii ya Kuondokewa na Tofauti zetu, na kupata Barka katika Mitizamo ya Macho yetu na kuwathamini Waislam wenzetu, kusikia kwetu na kutafakkari kwetu kwa ajili ya Dunia na Akhera yetu, kwa ajili ya Wazee wetu, familia zetu, wake zetu, watoto wetu n.k. Na bila ya shaka kuomba Toba na kua na shukrani kwa Neema alizotujaalia na kuzikubali na kuridhika nazo, ambako ndio kutakako tupelekea kusamehewa dhambi zetu na kuzidishiwa neema hizo na Mola wetu.

Na akasema *Ummu ul Muuminina* Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* alikua akiomba Dua ifuatayo katika Sala yake:**

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَ أَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الدَّجَّالِ وَ أَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَ الْمَمَاتِ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ الْمَأْثَمِ وَ الْمَغْرَمِ

Allahuma innee a`udhu bika min `adhabi 'l-qabri wa a`udhu bika min fitnati 'd-dajjal wa a`udhu bika min fitnati'l-mahya wa 'l-mamat, allahuma innee a`udhu bika min Al mathammi wa 'l-maghram.

*Tafsir**:***Ya Allah Hakika mimi naomba Hifadhi kutoka kwako dhidi ya Adhabu ya KaburiYa Allah Hakika Mimi naomba Hifadhi kutoka kwakoKutokana naMtihani wa Dajjal Na Naomba Hifadhi kutoka kwako Dhidi ya Mitihani Uhai na Mauti Ya Allah Hakika mimi naomba Hifadhi yako kutokana na kila aina ya Dhambi na Matatizo nisiyoyategemea**.(Muslim)*

Na kuna hadith isemayo:

عن قيس بن عباد، قال: صلَّى عمَّارُ بنُ ياسرٍ بالقومِ صلاةً أخفَّها ، فَكأنَّهم أنْكروها ! فقالَ : ألم أُتمَّ الرُّكوعَ والسُّجودَ ؟ قالوا : بلى ، قالَ أمَّا أنِّي دعوتُ فيها بدعاءٍ كانَ النَّبيُّ صلَّى اللَّهُ عليْهِ وسلَّمَ يدعو بِهِ اللَّهمَّ بعِلمِكَ الغيبَ وقدرتِكَ على الخلقِ أحيني ما علمتَ الحياةَ خيرًا لي وتوفَّني إذا علمتَ الوفاةَ خيرًا لي وأسألُكَ خشيتَكَ في الغيبِ والشَّهادةِ وَكلمةَ الإخلاصِ في الرِّضا والغضبِ وأسألُكَ نعيمًا لاَ ينفدُ وقرَّةَ عينٍ لاَ تنقطعُ وأسألُكَ الرِّضاءَ بالقضاءِ وبردَ العيشِ بعدَ الموتِ ولذَّةَ النَّظرِ إلى وجْهِكَ والشَّوقَ إلى لقائِكَ وأعوذُ بِكَ من ضرَّاءٍ مُضرَّةٍ وفتنةٍ مضلَّةٍ اللَّهمَّ زيِّنَّا بزينةِ الإيمانِ واجعَلنا هداةً مُهتدين.

Qays Ibn Abadi kua anasema kua: Alitusalisha Amar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* Sala ambayo ilikua ni Fupi sana. Hivyo Watu wakamlaumu kutokana na Ufupi wa Sala hio. Ambapo nae akawaambia Watu hao kwa kusema: 'Hivi jee Sikukamilisha mimi Rukuu zangu na Sujud zangu ndani yake? Na Jee sikusoma Dua aliyokua akisoma *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani yake?' Ambayo ni:

***Allahuma BiaAilmika Al Ghaybi wa Qudratika* - Ya Allah kwa Ilm yako ya Ghayb na Qudra zako Aala Khalqi - Juu ya Viumbe.**
***Ahyinii Ma Aalamta Al Hayata Khairan Li*- Nijaalie Niendelee Kuishi Kama Unajua kua Kuendelea Kuishi ni Bora Kwangu mie.**
***Watawfanii Idha Aalamta Alwafat Khayran* - Na ichukue Roho Yangu kama unajua kua Kufariki kwangu ni Kheri kwangu.**
***Wa As-aluka Khashyatika fi Al Ghaybi Wa Al Shahadati*- Na Nnakuomba (Unisamehe) kwa Kukhofia juu yako kutokana na Yasiyojulikana na Yanayojulikana.**
***Wa Kalimati Al Ikhlasi fi Al Rridhaa wa Al Ghasbi* - Na Nijaakie Kauli Iliyojaa Ikhlasi katika Wakati ninapokua na Furaha ninapokua na Hasira.**
***Wa As-aluka Naima la Yanfud* - Na Nakuomba Unijaalie Neema isiyokua na Mwisho na Furaha isiyokatika.**
***Wa Qurrat Ayni la Tanqut-aA'u* - Na nijaalie Kupata Utulivu wa Macho yangu usiokua na Mwisho.**
***Wa As-aluka Ridhaa bi Al Qadhai* - Na Nakuomba unijaalie kua ni mwenye Kuridhika kutokana na Majaaliwa yako juu yangu.**
***Wa Barda Al Aaisha baada Al Mawt* - Na nijaalie - Na Nijaalie Maisha yenye Ubaridi Tulivu baada ya Kufa kwangu**
***Wa Ladhat Al Nadhara ila Wajhika* - Na Nijaakie Nionje Ladha ya Kuona Muonekano wako**
***Wa Shawq Ila liqaika* - Na Hamu ya Kukutana nawe**
***Wa Aaudhubika kin Dharrai Mudhirrat* - Na Nakuomba unaiepushe na Madhara yenye Kudhuru**
***Wa Fitnati Mudhilati* - Na Mitihani yenye kudhadhalilisha**
***Allahuma Zayyina Biziynati Al imaani* - Ya Allah Tupambe na Mapambo yaliyojaa Imani**
***Waj-aAlnaa Hudata Muhtadiin* - Na Tujaalie tuwe Waongozi wa Waliongozwa katika Muongozo wako**.'*(Sunan An Nasai, Musnad Imam Ahmad)*

Naam..hii ni hadith inayoelezea pia Miongoni mwa Duaa ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alizokua akiziomba na pia kuwafundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhu* Kusoma Dua hizo katika Sala zao baada ya Tahiyyat kabla ya Salam.

Ambapo mbali ya kua Sala hio aliyosalisha Amar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* ilionekana kua Fupi lakini ilionekana kua ni yenye kujaa Manufaa makubwa ndani yake kutokana na Kisomo cha Dua yake baada ya Tahiyyat yake kabla ya Salam ya Sala yake. Kwani ilikua ni Sala ambayo ni yenye Dua iliyojaa Ucha Mungu ndani Ndani yake.

Na Miongoni mwa Duaa ambazo ni Rahisi sana kuomba kwa wale wenye uzito wa kutojua kuomba kwa Lugha ya Kiarabu, basi ni ile iliyoelezewa katika Hadith ya Abu Saleh ambayo inasema kua:

Amesema Mmoja kati ya Masahaba *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwambia mmoja kati ya Masahaba zake kwa kusema: '*Hivi unakua unasema Dua gani kwenye Sala yako?''

Hua Nnashuhudia kisha hua nasema*: 'Allahuma Inni As-aluka Al Jannati wa Audhubika Mina Nnar* - Ya Allah Hakika Mimi nakuomba Pepp na Uniepishe na Moto.'

Kisha Mtu huyo akaendelea kwa kusema: 'Lakini mimi sijui Dua uombazo wewe au aombazo Muadh.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Sisi Hua tunazungukia katika mambo hayo hayo katika kuomba'*(Musnad Imam Ahmad, Sunan Abu Daud)*

Kwani Katika Hadith hii tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomuuliza Kijana kuhusiana na Dua asomayo kwenye Sala yake, basi Kijana kajibu kua Anaomba Aingizwe Peponi na Aeupushwa na Moto.

Na kisha Kijana huyo akamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Lakini mimi sijui Kuomba kama Uombavyo Wewe na Muadh. Ambapo Kijana huyu alisema hivyo kwa Sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Mwenye Ilmu kubwa sana na m-bora wa kuomba Duakwani hua hasemi isipokua hua ni kutokana na Kushushiwa Wahyi na *Allah Subhanah wa Ta'ala* .

Na kwa upande wa Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* basi ni Sahaba Mwanazuoni mwenye Ilm kubwa Sana.Hivyo bila ya Shaka Mtu hua haiwezekana kujifananisha *na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na wala haiwezekani kujifananisha na Muadh.

Na ndio maana Kijana akajishusha chini na kusema kua yeye anaomba Vitu viwili hivyo tu na hajui zaidi mengine zaidi, na pia hajui Maneno anayotumia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Muadh Ibn Jabbal *Radhi Allahu Anhu* katika kuomba kwao.

Na amesema hivyo pia ili apate faida ya kujua kiombwacho na *Rasul Allah Salallhu Alayhi wa Salam*.
Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ikawa kama anamwambia: Usitaaabike kutaka kujua sisi tunaomba nini katika Dua zetu, kwani sisi pia katika Kuomba kwetu hua tinazunguka katika kuomba hayo hayo ya Kuingizwa Peponi na kuepushwa na Moto, na Hivyo Dua uiombayo inatosheleza.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Jambo la mwanzo atakaloulizwa Mja katika Siku ya Malipo ni kuhusiana hesabu yake litakua ni Sala yake**. **Hivyo Kama Sala yake itakua Salama basi Mtu huyo atakua amefuzu na kuokoka, lakini kama haitakua Salama basi Mtu huyo atakua amepotea na Kuangamia.'**(*Sunan An Nasai)*

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Pale mmoja wenu anapomaliza kusoma Tahiyyat ya Mwisho basi na Aombe Hifadhi kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*dhidi**

ya Mitihani ya Aina nne:Mtihani wa Moto wa Jahannam, Mtihani wa Adhabu ya Kaburi, Mitihani ya Uhai na Mauti na Mithani wa Masih Dajja*l.'**(Sahih Muslim)*

Ambapo Dua hio kwa Kiarabu hua inasomwa kama Ifuatavyo:
'***Allahuma Inni Audhubika* - Ya Allah Hakika Mimi naomba Hifadhi kutoka kwako Dhidi ya:**
***Min Adhaab Jahannam* - Kutokana na Adhabu ya Moto wa Jahannam.**
***Wa Min Adhabu Al Qabri* - Na Kutokana na Adhabu ya Kaburi.**
***Wa Min Fitnat Al Mahyaa wa Al Mamaat* - Na Kutokana na Mitihani ya Maisha na Mauti.**
***Wa Min Sharri Fitnat Al Masih Dajjal* - Na kutokana na Shari ya Mtihani wa Masih Dajjal.'**

Naam..hivyo hizo ndio baadhi ya Dua ambazo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifundisha, akipendekeza na pia Alizifurahia baada ya kuzisikia kutoka kwa Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum.*Na bila ya Shaka Duaa hua ni Sehemu Muhimu ya Sala,Kwani Neno Sala lenyewe hua linamaanisha Dua pia kwa upande mwengine, hivyo kila mmoja wetu asipoteze nafasi hii ya kuomba ndani ya Sala yake baad ya Tahiyyat ya mwisho kabla ya kutoa Salam.

Kwani kuacha kusoma Dua ndani ya Sala baada ya Tahiyyat ya mwisho hua ni sawa na livyosema Hujjat Ul Islami Mujaddid Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi kua: '**Watu wataenda Pwani kutafuta Chaza (Oyester), na Watapata Chaza, lakini ni wale watakaozifungua tu Chaza hizo ndio watakaonufaika na Lulu zilizomo ndani ya Chaza**. **Hivyo bila ya shaka Kama Chaza itakua ni Sala basi Lulu za Sala hua ni Kuomba Dua ndani yake**.'

Kwani amesema Jubayr Ibn Nufayr kua: **'Mimi nilimisikia Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* akisema Mwishoni mwa Sala zake baada ya Tahiyyat Kabla ya Taslim kua;**
Allahuma inni Aaudhubika Mina Al Khushui Al Nifaq - Ya Allah Kwa hakika mimi Nnajilinda kwako Dhidi ya Utiifu kwa Kinafiq.'

Ambapo anasema Muhammad Ibn Saad kua: '**Nilimiskia mimi Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* akisema kua:Jitahidini Kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* akulinde Dhidi ya Utiifu wa Kinafiq.'**

Hivyo Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* akaulizwa: Jee Khushuu ya Kinafiq ndio ipi?

Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu* akasema: Ni Pale Unapoona kua mwili wako Una Utiifu Mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala lakini* Moyo wako hauna Utiifu.'*(Shuab Al Iman)*

Naam..hadith inatuonesha namna Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walivyokua wakiiuogopa Unafiq kiasi ya kua Walikua wakiomba Kukingwa nao hadi ndani ya Sala zao.Na hivyo pia kutuonesha aina za Dua zinazoruhusika kuombwa baada ya Tahiyyat ndani ya Sala na umuhimu wake.Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: '**Hua inapendekezwa sana baada ya Salat Ibrahimiyyah kuomba Kitu chochote kile akitakacho mtu cha Kidunia na Kiakhera, na Imam Abu Muhammad amesema kua haifai kuomba Dua kwa kusema**:**Ya Allah Nijaalie Mimi nipate Mke mwenye Maumbile na sifa kadhaa wa kadhaa**. **Kwani hii hua inabatilisha Sala, hivyo Mtizamo Sahih ni kua Wengi miongoni mwa Wanazuoni**. **Wanasema kua Inaruhusika kuomba Dua zote za Halali, ila kuomba zile zilizotajwa kwenye Hadith hua zinapendekezwa zaid**i'*(Rawdat Talibin)*

Na akasema pia Shaykh Ul Islami Al Allamah Al Imam Shams Ad Din Al Ramli Al Shafii kua: '**Hua inapendekezwa baada ya Salat Ibrahimiyyah ndani ya Tahiyyat ya mwisho kuomba akitakacho Mtu iwe kwa Kidini au kwa Kidunia.'*****(****Nihayat Al Muhtaj)*

Na akasema pia Imam Abu Al Barakaat Al Dardir kua: '**Inapendekezwa Kuomba Dua baada ya Tashahhud ya Tahiyyat ya Mwisho na Salawat Ibrahimiyah.'**(*Sharh Al Kabir)*

Na kwa Upande wa Al Shaykh Ul Islami Al Aalamah Al Imam Zakarriyah Al Ansari Al Shafii kua:**'Inapendekezwa kuomba Dua baada Salat An Nabii na Salat Ibrahimiyyah katika Tahiyyat ya mwisho, kwa kile akitakacho Mtu husika kuhusiana na Mambo ya Kidunia na Kiakhera**. **Na hii ni kulingana na Hadith iliyomo katika Sahih Muslim iliyosema:Anapokaa Mmoja wenu katika Sala basi na Asome Tahiyyat hadi Mwisho kisha na achague kutoka katika Maombi ayatakayo na aombe.'***(Asna Matalib)*

Ambapo kwa upande wa Madhhb ya Imam Abu Hanifa basi inasema Al Majmuu Al Anhar Sharh Multaqa Abhur kua: '**Dua hua ni Sunnah ya Maombi yanayofuata baada ya Tahiyyat ya Kikao cha Mwisho kwa ajili ya kujiombea yeye mwenyewe anaesali na Wazee wake n.k kama Wazee hao ni Waislam na kuwaombea Waislam wote kwa ujumla.Na hii ni kulingana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliposema, Wakati anaposali mmoja wenu basi na aanze kwa kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha Asali na kisha amalizie kwa Maombi.'**

Na akasema Imam Ahmad Zarruq Al Maliki kua: '**Kulingana na Msingi wa Sharia basi hua inaruhusika kufanya Dhikr na kuomba Dua yoyote ambazo maana yake hua inakubalika baada ya Salat Ibrahimiyyah.'***(Al Qawaid)*

Ambapo Imam An Nawawi amerudia tena kusema katika Al Adhkar kua: '**Fahamu kua Dua hii baada ya Salat Ibrahimiyyah hua ni Sunna inayopendekezwa na hivyo hua si Wajib. Na hua inapendekezwa kurefushwa,isipokua pale Mtu atakapokua ni Imam, hivyo Mtu anaruhusika kuomba akitakacho kidunia na kiakhera**. **Na anaweza kuomba kwa Kutumka Dua za Kwenye Sunnah A Hadith na pia kwa Dua atakazozivumbua yeye mwenyewe, ila za kwenye Hadith hua ni Bora zai**d.'*(Al Adhkar)*

Na Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani akasema: '**Kuna Uthibitisho wa kukubalika kuvumbua Dua zako kwenye Sala ambazo hazitokua zikiendana Kinyume na Dua za Kwenye Hadith.'***(Fat-h Al Bar)*

Na Imam Al Shawqani Al Hanbali akasema: '**Inaruhusika kuomba Dua uitakayo ndani ya Sala baada ya Tahiyyat, iwe kuhusiana na Akhaera au Kidunia, iwe Fupi ama Ndefu,hatolaumika mtu kwa kuomba kwake pale itakapokua maombi hayo hayajumuishi Dhambi ndani yak**e.'*(Tuhfah Dhakiriin)*

12-TASLIM – KUTOA SALAM

❖❖❖❖

Naam tunarudi katika hadithi yetu isemayo:

حَدَّثَنَا سُوَيْدُ بْنُ سَعِيدٍ، حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ مُسْهِرٍ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ، طَرِيفٍ السَّعْدِيِّ ح وَحَدَّثَنَا أَبُو كُرَيْبٍ، مُحَمَّدُ بْنُ الْعَلاَءِ حَدَّثَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ السَّعْدِيِّ، عَنْ أَبِي نَضْرَةَ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ

الْخُدْرِيِّ، عَنِ النَّبِيِّ ـ صلى الله عليه وسلم ـ قَالَ " مِفْتَاحُ الصَّلاَةِ الطُّهُورُ وَتَحْرِيمُهَا التَّكْبِيرُ وَتَحْلِيلُهَا التَّسْلِيمُ "

Amesema Suwaidu Ibn Said kua amesema Aliyyu Ibn Mus-hir kua amesema Abi Sufyan kua amesema Taririf Ibn Saidi kua amesema Abi Nadhrat kua amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Ufunguo wa Sala ni Udhu, Kuingia ndani yake ni kwa Allahu Akbar na kuifunga kwake ni kwa Salam*(*Sunnan At Tirmidhii, Sunnan Abu Daud,Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Mtizamo wa Madhhab yetu (ya Imam Al Shafii) ni kua Taslim ni Wajib na hivyo hua ni Nguzo ya Sala ambayo ikikosekana basi Sala husika hua ni Batili**. **Na huu ndio Mtizamo wa wengi sana miongoni mwa Wanazuoni wa Masahaba, Tabiina na Tabii Tabiina na Waliofuatia baada yao.'***(Al Majmuu)*

Naam..kwa maana hio basi Taslim yaani Kusema *As Salaam Alaykum wa Rahmat Allahi wa Barakatuh* baada ya Tahiyyat ya Mwisho na baada ya Dua hua ni Nguzo ya 12 ya Sala.Ambapo *Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam* Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yanya An Nawawi anatuelezea Hikma iliyomo ndani ya Nguzo hii ya kufungia Sala, yaani Kumalizia Ibada ya Sala na kutoka nje yake kwa kusema kua:

'Wakati Mtu anaekua Imam anaposali na anapotoa Salam, basi hua na nia ya Kutoka Nje ya Sala kwa Salam ya kwanza,huku akiwa ni mwenye Kuwasalimia Malaika walioko katika upande wa Mkono wake wa Kulia ambao ni wenye kuandika Amali njema za Waja. **Na anapotoa Salaam ya pili katika Upande wa Kushoto hua na nia ya Kuwasalimia Malaika wanaoandika amali mbovu.**

Ambapo Kwa Mtu aliekua Maamuma anaposali na akatoa Salaam ya kwanza basi hua na nia ya Kuashiria Kutoka Nje ya Sala na pia Kumsalimia Imam, Kwa Malaika wanaoandika Amali zake, kwa Waliomzunguka katika Ibada ya Sala, pembeni yake, katika Safu yake mbele yake na Nyuma yake.

Na Salam ya pili hua na nia ya kuwasalimia Maamuma wenzake na Imam kama yupo mbele yake. Na hata kama akifanya Taslim (akitoa Salam) bila ya kua na Nia hizo basi hua inaruhusika na hii kwa sababu kuwatolea Salam watu waliokuzunguka au waliokuwepo mbele yako hua ni Sunna.Ama kwa anaesali Peke yake basi hua na nia ya Salam ya kwanza kwa Malaika wa Kulia na Salam ya pili kwa Malaika wa Kushoto.

Kwani Msingi wa Kanuni hii ni kutokana na Hadith ya Jabi Ibn Samura *Radhi Allahu Anhu* aliesema kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituamrisha sisikujitumia Salam sisi wenyewe na kusalimiana na wengine kwa Salaam (Al Majmuu)

Ambapo amesema Jabir Ibn Samura *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Tulipokua tukisali na *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* tulikua tukisema *As Salaam Alaykum wa Rahmat Allah, As Salaam Alaykum wa Rahmat Allahi*.Huku tukiashiria pande zote mbili kwa mikono yetu**. **Lakini Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema: Kwanini Mnaashiria kwa kupunga mikono yenu kama Mikia ya Farasi aliepumzika?**

Kwani hua inatosheleza kwa Mtu kuweka Mikono yake kwenye Mapaja yake huku akiwa ni mwenye kumsalimia Ndugu yake wa upande wa Kulia na Kushoto.

Ambapo Maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yasemayo 'Kumsalimia Ndugu yake wa Kulia na Kushoto yanamaanisha kuwasalimia Waislam wenzake anaosali nao, walioko kulia kwake na kushoto kwake.'*(Al Majmuu)***

Kwani amesema Hibanu Ibn Musa kua amesema Abd Allah kua amesema Muamar kua amesema Al Zahri kua amesema Mahmud Ibn Rabiyyah kua amesema Itban Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Sisi tulikua tukimalizia Sala zetu pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* kwa Salam.'

Na amesema Ummu Ul Muuminina Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua ni Mwenye kutoa Salam Moja tu katika wakati anaposali na hua pale anapokua ameelekea mbele na kugeukia kidogo Kulia.'***(Jamii Al Tirmidhii)***

Kwani Ingawa tumeona kua Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi amezungumzia kuhusiana na Taslim ya Sala kwa kutoa Salam mara mbili, kwa Upande wa Kulia na kushoto, ambapo amesema kua Kutoa Salam mara moja kwa Upande wa Kulia hua ni Wajib kwani kufanya hivyo hua ni Nguzo ya Sala lakini pia hua inapendekewa kutoa Salam mara ya pili pia kwa upande wa kushoto, ambapo huo ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na hii ni kulingana na Uthibitisho wa Hadith ya Jabir Ibn *Samura Radhi Allahu Anhu.*

Lakini kwa upande mwengine basi kuna Wanazuoni wanaosema kua inavyotakiwa hua ni Kutoa Salam moja tu, ambayo ni Nguzo ya Sala na hutolewa kwa upande wa Kulia tu.Na miongoni mwa Wanazuoni wenye Mtizamo huo ni Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik, Madhhab ya Ibadhi n.k.

Ambao wao Mtizamo wao unaegemea katika Uhtibitisho wa moja kati ya Hadith tulizoanza nazo leo yambayo ni ya Ummu Ul Muuminina Aisha *Radhi Allahu Anhu.*

Na Ingawa Hadith hii ni Hadith Sahih kulingana na Mtizamo wa Imam Al Hakim Al Nishapuri ambae amesema kua: **'Hii ni Hadith sahih kulingana na Vigezo vya Imam Bukhari na Muslim.'**

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Al Hafidh Al Imam Adh Dhahabi na Wanazuoni wengineo, lakini hata hivyo kwa upande mwengine basi Kuna Wanazuoni wasemao kua Hadith hii ni Dhaif.

Kwani kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik ambao ni Miongoni mwa wenye kusimamia kwenye Mtizamo wa Kutoa Salam Moja tu basi wao wanasema kua: '**Hua inapendekezwa kwa Maamuma anapotoa Salam kua ni mwenye kumtolea Salam Imam alieko mbele yake, lakini kwa Kimya kimya, bila kugeuza kichwa chake upande wa Imam. Na pia kama kuna Maamuma mwenzake anaesali nae ambae amekaa Kushoto kwake basi pia na amtolee Salam kimya kimya bila kugeuza Uso.'**

Kama alivyosema Mwanazuoni Mahiri wa Madhhab ya Imam Maliki aitwae Imam Ahmad Al Dardir Al Maliki katika Sharh Al Kabir kua: '**Na Sunna ya 11 ya Sala ni kua Maamuma anatakiwa Kumrudishia Salam Imam wake kimya kimya ndani ya Moyo wake na bila kumgeuzia kichwa**. **Na pia hua ni Sunna kumsalimia Kimya kimya Uliesali nae aliekaa katika Upande wa Kushoto yako, hata kama atakua ni Mtoto Mdogo.'**

Hivyo ingawa kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Al Imam Al Shafii basi tunaona kua katika kumakizia na Kutoka nje ya Sala baada ya Kisomo cha Tahiyyat basi hua inatakiwa Taslim mbili.Ambapo Taslim yaani *Salaam Alaykum wa Rahmat Allah* ya kwanza kwa kugeukia kidogo upande wa Kulia yako hua ni Wajib na Ni Nguzo miongoni mwa Nguzo za Sala.

Na Taslim ya Pili kwa kumalizia Salam kwa upande wa Kushoto hua ni Sunna Muakkadah yaani Sunna inayotiliwa mkazo kama alivyosema Imam An Nawawi.Ambapo Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kama alivyosema Imam Ali Al Shurunbulali na Imam At Tahawi pia kama ilivyoelezewa katika *Hashiyyah Maraqi Al Falah.*Na Imam na Maamuma wote hutakiwa kutoa Salam mbili katika Sala zao.

Na pia kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik basi kama tulivyoona kua wao wanasema kua Taslim ni Moja tu ambayo ni ya Kwanza inayotolewa katika Upande wa Kulia na Imam. Ambapo kwa upande wa Maamuma basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanasema kua yeye anatakiwa kutoa Salam Tatu, Moja upande wa Mbele yake yaani kwa Imam au, ya pili Kulia na ya tatu kushoto kwake.

Lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: **‘Taslim zote mbili za Kulia na Kushoto hua ni Wajib na ni Nguzo ya Sala. Na Hivyo Taslim ya pili hua si Lazima na ni Sunna katika Sala ya Maiti, Katika Sijda ya Kisomo na Sijda ya Shukrani. Moja upande wa Mbele yake yaani kwa Imam au, ya pili Kulia na ya tatu kushoto kwake.’**

Na pia kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua:**‘Taslim zote mbili za Kulia na Kushoto hua ni Wajib na ni Nguzo ya Sala. Na Hivyo Taslim ya pili hua si Lazima na ni Sunna katika Sala ya Maiti, Katika Sijda ya Kisomo na Sijda ya Shukrani.’**

Na tunaporudia kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao Wanasema kua: **‘Mtizamo wa kua Taslim hua ni Moja tu ni Mtizamo wa Watu wa Madina na Mtizamo wa Taslim mbili ni Mtizamo wa watu wa Iraq.’**

Ambapo Hadhith juu ya Taslim Moja imenukuliwa pia na Abd Allah Ibn Umar na Saad Ibn Saadi *Radhi Allahu Anhum* katika Musnad Imam Ahmad. Na Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii basi amesema kua: Mtizamo wa Taslim moja ni Mtizamo wa Masahaba na Muhajirina.

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ حُسَيْنٍ الدِّرْهَمِيُّ، حَدَّثَنَا ابْنُ أَبِي عَدِيٍّ، عَنْ بَهْزِ بْنِ حَكِيمٍ، حَدَّثَنَا زُرَارَةُ بْنُ أَوْفَى، : أَنَّ عَائِشَةَ، – رضى الله عنها – سُئِلَتْ عَنْ صَلاَةِ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فِي جَوْفِ اللَّيْلِ، فَقَالَتْ : كَانَ يُصَلِّي صَلاَةَ الْعِشَاءِ فِي جَمَاعَةٍ، ثُمَّ يَرْجِعُ إِلَى أَهْلِهِ فَيَرْكَعُ أَرْبَعَ رَكَعَاتٍ، ثُمَّ يَأْوِي إِلَى فِرَاشِهِ وَيَنَامُ وَطَهُورُهُ مُغَطًّى عِنْدَ رَأْسِهِ، وَسِوَاكُهُ مَوْضُوعٌ حَتَّى يَبْعَثَهُ اللَّهُ سَاعَتَهُ الَّتِي يَبْعَثُهُ مِنَ اللَّيْلِ، فَيَتَسَوَّكُ وَيُسْبِغُ الْوُضُوءَ، ثُمَّ يَقُومُ إِلَى مُصَلاَّهُ فَيُصَلِّي ثَمَانِ رَكَعَاتٍ يَقْرَأُ فِيهِنَّ بِأُمِّ الْكِتَابِ وَسُورَةٍ مِنَ الْقُرْآنِ وَمَا شَاءَ اللَّهُ، وَلاَ يَقْعُدُ فِي شَىْءٍ مِنْهَا حَتَّى يَقْعُدَ فِي الثَّامِنَةِ، وَلاَ يُسَلِّمُ، وَيَقْرَأُ فِي التَّاسِعَةِ، ثُمَّ يَقْعُدُ فَيَدْعُو بِمَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَدْعُوَهُ، وَيَسْأَلُهُ وَيَرْغَبُ إِلَيْهِ وَيُسَلِّمُ تَسْلِيمَةً وَاحِدَةً شَدِيدَةً، يَكَادُ يُوقِظُ أَهْلَ الْبَيْتِ مِنْ شِدَّةِ تَسْلِيمِهِ، ثُمَّ يَقْرَأُ وَهُوَ قَاعِدٌ بِأُمِّ الْكِتَابِ، وَيَرْكَعُ وَهُوَ قَاعِدٌ، ثُمَّ يَقْرَأُ الثَّانِيَةَ فَيَرْكَعُ وَيَسْجُدُ وَهُوَ قَاعِدٌ، ثُمَّ يَدْعُو مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَدْعُوَ، ثُمَّ يُسَلِّمُ وَيَنْصَرِفُ، فَلَمْ تَزَلْ تِلْكَ صَلاَةَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله

عليه وسلم حَتَّى بَدَّنَ فَنَقَصَ مِنَ التِّسْعِ ثِنْتَيْنِ، فَجَعَلَهَا إِلَى السِّتِّ وَالسَّبْعِ وَرَكْعَتَيْهِ وَهُوَ قَاعِدٌ حَتَّى قُبِضَ عَلَى ذَلِكَ صلى الله عليه وسلم

Kwani amesema Ali Ibn Husayn Al Dirhamy kua amesema Ibn Abi Adiy kua amesema Bahzi Ibn Hakim kua amesema Zurarah Ibn Awfah kua: 'Aisha *Radhi Allahu Anha* aliulizwa kuhusiana na Sala za Usiku na Qiyam Al Layl za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, Ambapo nae akasema:Alikua *Rasul Allah Salallahu Alayh wa Salam* akisali Sala ya Isha Msikitini, na kisha hurudi nyumbani kwake na kusali Rakaa nne.

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huingia Kitandani na kulala,huku Maji ya kutilia Udhu yakiwa yamewekwa na kufunikwa karibu na Kichwa chake, Na Msuwaki wake huwekwa pembeni yake, hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapomuamsha katika Usiku huo. Anapoamka, husugua meno, kisha hutia Udhu kisha hukaa katika sehemu yake ya kusalia na kisha Husali Sala ya Rakaa Nane.

Ambazo ndani yake husoma Surat Al Fatiha na Sura nyenginezo za Qur'an anazojaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuzisoma.Na wala alikua hapumziki baina yale Rakaa hizo hadi baada ya Rakaa ya Nane. Na alikua hatoi Salam bali alikua ni mwenye kusoma Qur' katika Rakaa ya Tisa, Na kisha Hubakia kumuomba sana *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kadri awezavyo. Na Kuomba Dua na Kumnyenyekea, na kisha Hutoa Salam Mara moja kwa sauti kiasi ya Kua hata Watu waliolala Ndani ya Nyumba huweza kuamka kwa Salam yake hio.

Na kisha Husoma Sura Al Fatiha huku akiwa amekaa Kitako, Hurukuu huku akiwa amekaa Kitako, Husjudu huku akiwa amekaa Kitako, kisha Husoma tena Qur'an katika Rakaa ya Pili. Na kisha Hurukuu na Kusujudu huku akiwa amekaa Kitako na kisha Husoma Tahiyyat na Kuomba Dua na kisha Hutoa Salam Mara moja na kugeukia upande wa Kulia.

Hivi ndivyoilivyokua wingi wa Sala za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hadi akaongezeka Uzito, na kisha akaanza kupunguza Rakaa mbili katika Tisa. Na akawa anaanza kusali Rakaa Sita na Saba akiwa amesimama na Rakaa mbili zilizobakia alizisali huku akiwa Amekaa Kitako, hadi kufaruki kwake.'*(Sunan Abu Daud)*

Ambapo hii ni miongoni mwa Hadith ambazo zinatuonesha namna alivyokua Akisali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala zake za Usiku katika kipindi cha Mwishoni mwa Uhai wake.Ambayo ingawa ndani yake Sala hizi tunaona kua mlikua na Taslim moja tu ambayo ni kwa sauti.Lakini hata hivyo amesema Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri al Nishapuri hii kua:**'Abu Daud ameinukuu kutoka kwa Zurarah Ibn Awfa ambae ameinukuu kutoka kwa Saad Ibn Hisham ambae amenukuu kutoka kwa Aisha. Na akasema kua Huu sio ukamilifu wa Hadith. Kwani amesema Abu Hatim Al Razi kua: Amemnukuu Zurara kutoka kwa Imran Ibn Husayn, na kutoka kwa Abu Hurayrah na kutoka kwa Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhum* pia. Na hivyo ndivyo ilivyokua kuhusiana na ukweli wake kwani Zurarah Ibn Awfa hajawahi kunukuu kutoka kwa Aisha *Radhi Allahu Anha.***

Amesema Utba Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Sisi tulikua tukisali pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na tulikua tukimalizia Sala zetu kwa Taslim pamoja *nae'***(*Sahih Bukhari)*

Ambapo anasema Imam Abu Hanifa kulingana na Hadith hii kua: '**Hua ni Sunnah kwa Maamuma kutamka Salaam huku akiwa ni mwenye kufuatana na Salam ya Imam.'**(*Maraqi Al Falah)*

Na ingawa huo ni Mtizamo wa Imam Abu Hanifa lakini hata hivyo kaa upande wa Wanafunzi wake Wakuu Imam Abu Hanifa akiwemo Imam Abu Yusuf na Imam Muhammaf Ash Shaybani basi wao wanasema kua: **'Hua ni Sunna kwa Maamuma kutamka Salaam baada ya Imam Kutamka Salam.'***(Maraqi Al Falah)*

Na hivyo anasema Al Aalamah Al Muhakkik Imam Ibn Aabidin Ash Shami Al Hanafi kua: '**Kama Maamuma ikiwa hajamaliza Tahiyyat yake na kisha Imam Akatoa Salam basi Maamuma husika hutakiwa kumaliza Tahiyyat yake na mara tu baada ya kumaliza Tahiyyat hio basi anatakiwa nae atoe Salam**.'*(Rad Al Mukhtar)*

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Hua ni Bora zaidi kwa Maamuma anaesali Nyuma ya Imam asitoe Salam mwishoni mwa Sala yake hadi pale Imam wake atakapokua Tayari ameshamaliza kutoa Salaam ya Pili.***(Al Majmuu)*

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Muhammad Ibn Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Faraa Al Baghawi Al Shafii Basi yeye anasema kua: '**Mtu yeyote anaesali Nyuma ya Imam basi Wakati Imam anapomaliza kutoa Salam,basi na yeye Maamuma atoe Salam kulia kwake na kushoto kwake.Kwani Hua ni Mustahab (Inapendekezwa na Kutiliwa Mkazo)kua Maamua asitoe Salam hadi pale Imam awe ameshamaliza Kutoa Salaam Zote mbili,na huu ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii kulingana na kauli ya Al Buwayti.'**

Naam..kwa kua Imam amechaguliwa kwa ajili ya kufuatwa kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* basi Wanazuoni wanakubaliana kua hua ni Vizuri zaidi kwa Maamuma Kutoa salaam baada ya Imam wake kumalizia Salaam ya pili.Na hivyo basi Mtizamo wa Imam Abu Hanifa katika hili hua ni Mtizamo usiokua na Nguvu na Wanazuoni wanasema kua inakirihisha kwa Maamuma kutoa Salamsambamba na Imam ingawa kufanya hivyo hakubatilishi Sala ya Mtu.

Yaani afadhali zaid hua ni Kutoa Salam baada ya Imam kumalizia Salam ya kwanza na hivyo kua si mwenye kuenda nae sambamba au kumtangulia.

Kwani Kwa kua Kuna Makubaliano ya Wanazuoni juu ya Mtizamo wa Kua Taslim ya Kwanza hua ni Nguzo ya Sala, na hivyo Sala ya Mtu Husika uubatilika inapokosekana Taslim ya kwanza na kuna kutofautiana kuhusiana na Taslim ya pili kwani Wanazuoni wasemao kua haihitajiki, na kuna wanaosema kua ni Sunna Unayotiliwa Mkazo na pia kuna Wasemao kua ni Fardhi .

Basi Wanazuoni wanakubaliana pia kua Kutoa Taslim tu moja hua si kwenye kupelekea kubatilisha Sala Hivyo Kama Imam akiwa ametamka Taslim Moja tu na Maamuma ni mwenye kutaka Kutaka kufanya Taslim mbili basi hua hamna tatizo na hii ni kwa sababu hata hao Watumiao Taslim Moja wanasema kua hio ni kwa Imam lakini Maamuma anatakiwa afanye Taslim mbili kama tulivyoona hapo kabla kwenye Mtizamo wa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik.

Kwani amesema Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri kua: **'Wanazuoni wote ambao miminilisoma chini yao wanakubaliana kua, pale Mtu anaesali na kisha akamalizia Sala yake kwa Taslim moja tu, basi hua inakubalika, lakini ni Sunnah kutoa Salam kuanzia katika upande wa Kulia nakumalizia kwa upande wa kushoto, na hii ni kulingana na Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu'***

Na kuna hadith ismayo kua:

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ آدَمَ، عَنْ عُمَرَ بْنِ عُبَيْدٍ، عَنْ أَبِي إِسْحَاقَ، عَنْ أَبِي الأَحْوَصِ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ، قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يُسَلِّمُ عَنْ يَمِينِهِ حَتَّى يَبْدُوَ بَيَاضُ خَدِّهِ وَعَنْ يَسَارِهِ حَتَّى يَبْدُوَ بَيَاضُ خَدِّهِ .

Amesema Muhammad Ibn Adam kua amesema Umar Ibn Ubaydi kua amesema Abi Is-haq ua amesema Abi Al Ahwass kua amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allah Anhu* kua: **'Alikua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akitoa Salam katika upande wake wa kulia hadi weupe wa Shavu lake ulikua ukionekana na kwa upande wa kushoto kwake hadi weupe wa Shavu lake ulikua ukionekana.'***(Imam An Nasai)*

Ambapo tunaporudi kwa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi anaesema kua: '**Mtizamo wa Taslim Mbili ndio Mtizamo wa Madhhab yetu na wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni wa Masahaba na Tabiina na Tabii Tabiina kama alivyosema Imam Ibn Al Mundhiri kua Mtizamo huo ni wa Abu Bakr As Siddiq, Ali Ibn Abi Talib, Abd Allah Ibn Masud na Amar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhum.***

Mtizamo huu pia kwa Upande wa Tabiina ni wa Imam Ata Ibn Abi Rabah, Imam Alqamah, Imam Abd Rahman Al Sulami.

Na kwa Upande wa Tabii Tabiina ni wa Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Thawr na As-hab Al Ray yaani Wafuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Na kuna Wanazuoni ambao wanasema kua Taslim ni Moja tu. Ambapo huu ni Mtizamo wa Abd Allah Ibn Umar, *Radhi Allahu Anhu*, Anas Ibn Malik, Salamah Ibn Akwa na Aisha *Radhi Allahu Anhum.*

Na kwa Upande wa Tabiina ni Mtizamo wa Imam Hasan Al Basr, Imam Muhammad Ibn Sirin, Umar Ibn Abd Al Aziz, Imam Malik, na Imam Al Awzai.

Ambapo Imam Ibn Al Mundhiri amesema kua: Ammar Ibn Abi Ammar amesema kua: Katika Msikiti wa Ansar wa Madina, Basi Wao walikua wanapomaliza Kusali hutoa Taslim Mbili. Na katika Msikiti wa Muhajiriina basi wao walikua wakimaliza kusali hutoa Taslim Moja, Lakini Mimi mwenyewe (Imam Ibn Al Mundhiri) ni mwenye Kupendelea kutoa Taslim mbili.'

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kutuambia kwa kusisitiza kua: '**Mtizamo wetu sisi ni kua Taslim ya Kwanza hua ni Fardhi na Taslim ya Pili hua si Fardhi bali ni Sunna, na huo ndio Mtizamo wa Takriban Wanazuoni wote**, Ibn **Al Mundhir amesema kua: Wanazuoni Wanakubaliana kua Sala ya Mtu anaefanya Taslim Moja tu hua ni Sahih. At Tahawi, Al Qadhi Abu Tayyib na wengineo wamesema kua amesema Hasan Ibn Saalih kuhusiana na Taslim zote kua ni Fardhi, ambapo juu ya hili pia imenukuliwa kutoka kwa Ahmad Ibn Hanbal na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik.'***(Al Majmuu)***

13-TARTIB – KUFUATISHA UTARATIBU

Naam..Alhamd lillah tumeangalia kuhusiana na Nguzo 12 za Ibada ya Sala, moja baada ya nyengine kulingana na vithibitisho vya Aya, Hadith, na Mitizamo ya Wanazuoni kulingana na Madhhab yao katika Uislam.

Hivyo tunaingia katika Nguzo ya 13 inayojulikana kama Tartib Al Arqan wa Waradaha yaani: Kufuatisha Utaratibu wa Nguzo za Sala na Dhikr zake.Ambapo hua ni kulingana na kama alivyoamrisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Salini kama Milivyoniona Mimi nikisali'***(Sahih Bukhari)*

Kwani kama tulivyoelezea tangu mwanzoni kwa mpangilio na utaratibu wake hatua kwa hatua kuhusiana na Ibada ya Sala, mara baada ya kutia Udhu kua ni ni Lazima Kuitekeleza Ibada ya Sala kwa kufuata utaratibu ufuatao:

1-Kutia Nia
2-Kutamka Takbirat Al Ihram
3-Qiyyam - Kusimama
4-Qiraat Surat Al Fatiha
5-Ruquu
6-I'tidAl Kusimama baada ya Kurukuu
7-Sujud
8-Kukaa Kitako Baina ya Mbili
9-Kutulia baina ya Sijda Mbili
10-Tashahhud
11-Kukaa Kitako katika Tahiyyat ya Mwisho
12-Taslim
13-Tartib - Kufuatisha Utaratibu huu.

Kwa maana hio basi kama Mtu atasali Hata Sala ya Rakaa 1000 na yenye Khushuu kubwa Sana, lakini bila ya kufuata mpangilo huo, basi Sala yake yote hio hua ni Bure, kwani Hua si Sala. Kwa sababu Ili Sala iwe ni Sala basi inabidi iwe ni yenye kufuata Utaratibu alioufundisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hivyo kama Mtu atasali na hivyo kubadilisha Mpangilio kwa kuruka nguzo kati ya Nguzo za Sala kwa Kughafilika au Kusahau basi Kutokana na kua Mtu huyo amekiuka Mpangilio, hua ni lazima kwake kurudia sehemu ya Nguzo aliyoikiuka, kwa sababu sehemu yake hio ya Sala imekosekana, na hivyo ameshaharibu Utaratibu wa Mpangilio wa Nguzo ya Sala husika.

Kwa maana hio kama ikiwa Mtu hakugutuka kua ameiruka Nguzo ya Sala ya Rakaa husika hadi pale alipoingia katika Rakaa nyengine basi hio Rakaa iliyokiukwa Nguzo yake hua haihesabiki na hivyo atahesabu Rakaa aliyokuwepo kua ndio mbadala wake.

Yaani kama alikua Rakaa ya pili akaruka Nguzo ndani yake bila kukumbuka hadi alipoingia na kusimama katika Rakaa ya Tatu.Basi Rakaa yake hio ya Tatu itakua ni Rakaa ya pili kwake badala yake.Kwani kila hatua inatakiwa itekelezwa kama tulivyoelezea hapo kabla.

Naam..Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Kusimamia Utaratibu wa Mpangilio wa Kila Hatua ndani ya Sala basi hua pia tunazungumzia kuhusiana muunganisho wa maneno na vitendo katika hatua Husika katika Utaratibu wake.

Yaani kwa mfano, Kuiunganisha Nia ya Sala husika na Kutamka Takbirat Al Ihram huku ukiwa katika hali ya Kusimama kila asiekua na Dharura.

Kusoma Surat Al Fatiha huku ukiwa Umesimama, au Kusoma Tahiyyat huku ukiwa umekaa Kitako.n.k.

Kwani mbali ya kusahau na kughafilika lakini pia utaratibu huweza kuvunjika kama ikiwa Mtu atakua na Shaka labda kuhusiana na utekelezwaji wa Nguzo husika.

Yaani kwa mfano Mtu alikua anasali na kisha akaingia kwenye Rukuu,na kisha akaanza kujiuliza kama alisoma Surat Al Fatiha ama la, basi Mtu huyo hua anatakiwa asimame haraka sana kabla hajapata Utulivu ndani ya Rukuu yake hio.kwani akipata utulivu tu ndani yake basi inakua tayari ameshaingia ndani ya Nguzo nyengine na hivyo kila kitakachofuatia hapo baina ya rakaa hio hakitohesabika. Hivyo itambidi airudie Rakaa yake hio baada yake ndani ya Sala hio.Na Hukmu hii hua inamhusu mtu ambae ni mwenye Kusali peke yake.

Lakini kwa Mtu ambae ni Maamuma, anaemfuata Imam, na kisha akavunja Nguzo ya Sala au akawa na Shaka nayo Nguzo husika kama kaisimamisha ama la, basi Mtu huyo humbidi kuendelea na Sala yake huku akiwa ni mwenye Kumfuata Imam hadi Mwisho Imam Atakapotoa Salam na kisha yeye itambidi asimame kumalizia Rakaa Aliyoitilia shaka ya kuvunjikika kwa Nguzo yake.

Miongoni mwa mifano ya kupanguka kwa Utaratibu pia ni kama pale Mtu atakapokua ameenda chini Kusujudu lakini magoti yalipogusa Ardhi akawa na shaka kama alirukuu ama la kua basi hapo hapo anatakiwa arudi Juu kisha Arukuu na kisha anyanyuke ndio Asujudu.

Na tusema kama ikiwa Mtu hakurukuu katika wakati huo wa Kusujudu lakini akakumbuka katika wakati Rukuu ya Rakaa inayofuata kua kumbe Katika Rakaa Iliyotangulia hakurukuu, basi Rakaa yake iliyotangulia itafutika kwa kukosa Utaratibu na haitohesabika bali atahesabu Rakaa hio aliyokumbuka ndani yake kua ndio sawa na Rakaa iliyotangulia.

Na kama mtu akikumbuka katika Rakaa ya Nne kua katika Rakaa ya Pili hakurukuu, basi Rakaa yake hio ya nne itakua ni Rakaa yake ya Tatu badala yake.

Ambapo Mtu akisahau au akiwacha Nguzo basi Hua anairudia Nguzo hio na kisha Analeta Sijdat Sahw mwishoni mwa Sala

Na akisahau Sunna ya Sala basi hua Harudii Sunna bali hua analeta Sijdat Sahw mwishoni mwa Sala.

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Kusimamia Utaratibu wa Nguzo za Sala basi ndani yake hua pia mnaingia Kisomo cha Aya za Qur'an, hususan Kisomo cha Surat Al Fatiha.Hivyo Surat Al Fatiha katika Sala hua inatakiwa isomwe katika Mpangilio wake, herufi kwa herufi, neno kwa neno aya kwa aya.

Yaani kwa mfano Mtu atakaesoma Surat Al Fatiha na kisha katika Neno 'Iyyaka Naa'Abudu' ambapo neno Iyyaka hua ni lenye kutakiwa kulitia Mkazo kwa kuikaza herufi Ya. Hivyo kama Mtu akiwa hajatilia mkazo herufi Ya na akairegeza na hivyo ikawa amesema *'Iyaaka NaaA'budu* kwa makusudi, basi hua tayari ameshabadilisha maana na ameshakufuru na hivyo Sala yake imeshabatilika.Na hii ni

kwa sababu ya kua Neno *Iyaaka* hua linamaanisha Mwangaza wa Jua.Na kutokana na kusema kwake hivyo Mtu husika hua badala ya kusema Ni wewe tu ndie Tunaekuabudu basi hua Amesema Ni Mwangaza wa Jua ndio Tunaouabudu

Na Miongoni mwa herufi za Kiarabu zinazowachanganya watu katika Kutamka hua ni herufi *Sadd* ambapo wengi huitamka kama *Sin,* na wengine huitamka kama Swad.Mbali ya kua herufi Swad hua si herufu *Sin* wala si herufi *Sadd.*

Ambapo anasema Al Aallamah Shaykh Ul Islami Zayn Ad Din Imam Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Sunayki Al Ansari Al Shafii kua: '**Herufi *Al Asliyyah* Ni herufi zenye Sauti yenye kufanana na Mlio wa Mluzi wa Ndege ambazo hua zinatoka kwenye ncha ya Ulimi na hua ni herufi *'Sad',' Zay' na 'Sin'*.**

Na Mluzi wake Herufi hizi hua una aina ya Nguvu yake, na Herufi Sad ndio yenye Mlio wenye Nguvu zaidi katika Kukaza na Kupandisha kimatamshi.*(Al Jazarriyah)*

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii basi yeye amesema kua: **'Asili ya herufi hizi kuitwa *Asliyyah* ni kwa sababu *Asl* hua ni Mwiba mrefu wa Mti, na pia neno *Asl* hua linamaanisha Mshale.'**

Ama kwa Jarrah Allah Sultan Al Balagha Imam Abu Qasim Al Zamakhashari basi yeye anasema kuhusiana na herufi hizi kua: '***Asl* hua ni Mti ambao Matawi yake yanatumiwa kutengeneza Chujio, na Mshare pia huitwa *Asl* Na pia Mtu mwenye Ulimi mwepesi huitwa *Asl* pia.'**

Ama kwa upande wa Imam Muhammaf Ibn Mukarram Ibn Ali Ibn Ahmad Ibn Manzur Al Ansari Al Afriqi Al Misti Al Khazraji*Al Maliki* ambae ni mwandishi wa *Lisan Al Arabi* basi yeye anasema kua:
Herufi *Sad, Zay* na *Sin* ni herufi zenye kua na Sifa moja ya kua ni zenye kutoka kwenye msingi wa Ulimi na kutamkwa kwa Kutumia Ncha ya Ulimi, na herufi *Sad* hua haiambatani pamoja na Sin wala *Zay* katika Lugha ya Kiarabu. Na Herufi *Sad* hua ni Moja kati ya herufi 10 zenye utamkwaji wa Kimya kimya.

Na akasema Imam Abu Khayr Shams Ad Din Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Yusuf Al Jazari Al Shafii kua: '**Herufi za Mluzi ni herufi *Sad, Zay na Sin* ambazo hua zinatamkwa kwa kupitia kwenye Ncha ya Ulimi baina ya meno ya Mbele ya chini, hizi ndio Herufi Asilia kwani asili yake ni chini ya Ulimi uliochongo**ka**'***(Al Nashr)***

Hivyo Wanazuoni hua Wanakubaliana kua: '**Herufi Sad ni yenye Kutofautiana na heruf *Sin* na *Zay* kwa Sifa nne kuu Kimatamshi ambapo kwanza Herufi *Sad* hua ni yenye Kukazwa, hua ni ya Mnong'onezo, hua ni yenye Ukimya na hua ni yenye Kutamkwa kwa kuzibwa zibwa, Hivyo Inapotamkwa herufi Sad basi ncha ya Ulimi hunyanyuliwa na kuelekea juu kama kuuziba mdomo kwa ulimi.**

Herufi Sin inapotamkwa basi Ncha ya Ulimi huelekea Chini.

Na Herufi Zay inapotamkwa basi Ncha ya Ulimi hubakia kati kati ya mdomo.'

Kwa maana hio basi Mtu anaposoma Surat Al Fatiha na kisha akachanganya katika kutamka kwake herufi *Sad* tuseme katika Maneno *Ihdina Ssirata Al Mustaqiim,* ambapo neno *Sirata* limetumia herufi *Sad,* na akatumia herufi *Sin* badala yake basi hua tayari amebadikisha mpangilio wa aya, ameshabadilisha maana ya aya, na hivyo kisomo chake hua batili na Sala hua batili pia kama ikiwa mtu

huyo anajua hayo na kisha akafanya kwa makusudi, hivyo anatakiwa arudie aya hio. Kwa kuisoma kiusahih ili Sala yake isibatilike.

TMA'ININAH

❖❖❖

Neno *Tam'ana* kwa Lugha ya Kiaraju hua linamaanisha Kutegemea, Kutulia, Kuinama, Kupumzika, Kukaa kwa Utulivu, Kukaa kwa Usalama, Kukaa Kimyaa,Kua Salama, Kukaa kwa Kuridhia, Kutokua na Mwendo wowote.

Kwani wengi hua tunaitumia asili ya neno *Tam'ana* pale tunapozungumzia kuhusiana na aina za Nafsi katika *Nafs Mutmainah* yaani iliyotulia kwa Salama na Utulivu, Na pia kutokana na aya isemayo:

﴿ ألا بذكر الله تطمئن القلوب﴾

Ala Bi Dhikr Allahi Tatmainnat Al Quluub* - Kutokana na Dhikr Allah basi Nyoyo Hupata Utulivu(Surat Rad 13:28)*

Naam..hizo ni baadhi ya Mifano ya Aya zilizotumia asili ya neno *Tam'ana* yaani Utulivu wa Salama na Maridhiko.Ambapo hii ndio hali ambayo inayotakiwa kua nayo Mtu katika Ibada ya Sala kwani ndani yake hua mna *Dhikr Allah.*Na kwa kua Sala hua ni Ibada basi hali ya Utulivu ndani yake kutafutwa hua ni wa lazima kupatikana kwani kukosekana kwake hua ni kwenye kubatilisha Sala.

Hivyo Miongoni mwa Vitu vinavyobatilisha Sala hua ni Kufanya vitendo zaidi ya Vitatu katika Hatua moja ya Sala visivyojumuisha sehemu ya Sala ndani ya Sala.Kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi katika *Minhaj Talibin* kua:

'Kama ikiwa Mtu atafanya kwa Makusudi Kitendo ambacho hakihusiani na Sala ndani ya Sala basi Sala ya Mtu huyo hua ni yenye Kubatilika. **Isipokua kama itakua Mtu huyo amesahau, na kama Kitendo hicho kikiwa ni cha mara Nyingi basi pia Sala hubatilik**a.'

Na anasema Imam Shams ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini kua: '**Wingi na uchache wa Kitendo katika Sala hua ni Ule unaohesabika kwa usahih zaidi hua ni kulingana na Desturi za Watu husika, kwa mfano Kuvua Kiatu, kupiga kofi kumuua Mdudu mwenye Damu kidogo na kuvaa vazi ambalo ni rahisi sana kuvalika**. **Hivyo Kama kulingana na Desturi za watu juu ya moja kati ya mambo haya hua linahesabika ni dogo, basi hilo hua ni Dogo**.'*(Al Mughni Al Muhtaj)*

Ambapo tukirudi kwa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi basi yeye anafafanua zaidi kwa kusema kua: '**Kitendo huhesabika katika hali ya wingi pale kitendo husika kinapokua kinajumuisha idadi ya wingi wa mara tatu katika ufanywaji wake kitendo kimoja**. **Na kama kikiwa chini ya mara tatu kiidadi basi kitendo husika huhesabika kua ni kidogo**. **Na pia kama Vitendo vikiwa tofauti vimefanyika zaidi ya mara tatu basi hua si vingi kiidadi.'**

Yaani kwa mfano kitendo cha kupiga hatua mbili za Miguu na kisha Kurusha ngumi mara mbili hua ni vitendo viwili tofauti na hivyo huhesabika kua ni vidogo kiidadi mbali ya kua kwa pamoja kiidadi ni vinne kwani hatua mbili za miguu na ngumi mbili.

Hivyo Mtu anaesali hua anatakiwa atulie, na kujidhibiti kivitendo visizidi zaidi ya vitatu ili asibatilishe Sala yake.Ila kama itakua kuna dharura ya kufanya hivyo basi hua inaruhusika kutenda kwa mara mbili kwa aina moja na mara nyengine kwa aina nyengine na hivyo kutobatilisha Sala yake.

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na *Tmaaniinah* ambayo hua ni Hali ya Utulivu katika Sala, basi hua tunazungumzia moja kati ya Nguzo za Sala ambayo hua ni Nguzo ya 14.Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik,Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wanakubaliana kua Nguzo ya Sala na ni Wajibu wa Mtu Mwenye Kusali kuutekeleza.

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao Wanasema kua *Tmaaniinah* hua ni Wajib wa Kila Hatua ambayo ni Nguzo ndani ya Sala inayosaliwa na Mtu mmoja peke yake.

Na amesema pia Imam Abu Hanifa kua: **‘Amesema Malik kua kukaa katika hali ya Utulivu baina ya Sijda mbili hua si Fardhi ,bali kama mtu akishuka moja kwa moja kutoka kwenye Rukuu na kisha akasjudu au akanyanyua kichwa chake kidogo tu basi hua inatosheleza’**

Nauthibitisho wa Imam Abu Hanifa ni katik aya isemayo:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱرۡكَعُواْ وَٱسۡجُدُواْ وَٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمۡ وَٱفۡعَلُواْ ٱلۡخَيۡرَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Hajj 22:77)*

*Tafsir: **Enyi Wale ambao Mlioamini Rukuuni na Sujuduni Na muabuduni Mola wenu Na Fanyeni Mambo ya Kheri Ili Mpate kua ni wenye Kufuzu**.*

ingawa Wanazuoni Wanatumia uthibitisho wa hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* aliyosema kua:

قَالَ رِفَاعَةُ وَنَحْنُ مَعَهُ إِذْ جَاءَهُ رَجُلٌ كَالْبَدَوِيِّ فَصَلَّى فَأَخَفَّ صَلاَتَهُ ثُمَّ انْصَرَفَ فَسَلَّمَ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَقَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَرَجَعَ فَصَلَّى ثُمَّ جَاءَ فَسَلَّمَ عَلَيْهِ فَقَالَ " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَفَعَلَ ذَلِكَ مَرَّتَيْنِ أَوْ ثَلاَثًا كُلُّ ذَلِكَ يَأْتِي النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم فَيُسَلِّمُ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَيَقُولُ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " وَعَلَيْكَ فَارْجِعْ فَصَلِّ فَإِنَّكَ لَمْ تُصَلِّ " . فَخَافَ النَّاسُ وَكَبُرَ عَلَيْهِمْ أَنْ يَكُونَ مَنْ أَخَفَّ صَلاَتَهُ لَمْ يُصَلِّ فَقَالَ الرَّجُلُ فِي آخِرِ ذَلِكَ فَأَرِنِي وَعَلِّمْنِي فَإِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ أُصِيبُ وَأُخْطِئُ . فَقَالَ " أَجَلْ إِذَا قُمْتَ إِلَى الصَّلاَةِ فَتَوَضَّأْ كَمَا أَمَرَكَ اللَّهُ ثُمَّ تَشَهَّدْ وَأَقِمْ فَإِنْ كَانَ مَعَكَ قُرْآنٌ فَاقْرَأْ وَإِلاَّ فَاحْمَدِ اللَّهَ وَكَبِّرْهُ وَهَلِّلْهُ ثُمَّ ارْكَعْ فَاطْمَئِنَّ رَاكِعًا ثُمَّ اعْتَدِلْ قَائِمًا ثُمَّ اسْجُدْ فَاعْتَدِلْ سَاجِدًا ثُمَّ اجْلِسْ فَاطْمَئِنَّ جَالِسًا ثُمَّ

قُمْ فَإِذَا فَعَلْتَ ذَلِكَ فَقَدْ تَمَّتْ صَلاَتُكَ وَإِنِ انْتَقَصْتَ مِنْهُ شَيْئًا انْتَقَصْتَ مِنْ صَلاَتِكَ " . قَالَ وَكَانَ هَذَا أَهْوَنَ عَلَيْهِمْ مِنَ الأَوَّلِ أَنَّهُ مَنِ انْتَقَصَ مِنْ ذَلِكَ شَيْئًا انْتَقَصَ مِنْ صَلاَتِهِ وَلَمْ تَذْهَبْ كُلُّهَا.

Amesema Rifaa Ibn Rafii *Radhi Allahu Anhu* kua, Siku moja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua amekaa Msikitini nasi tukiwa pamoja nae.

Na mara akaingia Bedui alieonekana kama kwamba anataka Kusali, na Kasali Sala yake kwa Ufupi sana, na kisha alipomaliza akanyanyuka na kumsalimia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akitikia *Wa Alaykum Salaam* na kisha akasema: 'Rudi ukasali tena, kwani kwa hakika wewe Hujasali.'**

Hivyo yule Bedui akarudia Kusali kisha akamsalimia tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akamuitikia na kisha akamwambia Rudia tena kusali kwani kwa hakika wewe hukusali.

Bedui akarudia Kusali na kurudishwa kama mara mbili tatu na kila mara *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anamwambia Arudie kusali.

Tukio hili liliwashtua Sana Masahaba kutokana na kuona kua kumbe Mtu anaesali Sala fupi hua hana sala.

Lakini mwishowe Bedui huyo akasema: '*Ya Rasul Allah,* basi bora nifundishe kwani mimi ni Ibn Adam mwenye kujihangaisha na kukosea.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Sawa Unapotaka kusali tia Udhu kama alivyokuamrisha *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kisha Adhini na Kimu Sala pia.**

Kisha Ukisali basi Soma Qur'an kama unajua na kama hujui basi Mtukuze *Allah Subhanah wa Ta'ala,* fanya *Dhikr Allah* na fanya *Tahlil,*Kisha Rukuu hadi uwe umetulia kwenye Rukuu yako, kisha Simama Sawia,kisha Sujudu kikamilifu, kisha Kaa kitako hadi uhakikishe kua umepumzika,Kisha Simama na ukifanya hivyo utakua umekamilisha Sala yako, na ukipunguza basi utakua hukuikamilisha Sala yako.

Na Hivyo hua ni bora kuliko kutokamilisha, kwani ikipungua kitu Sala yako basi itakupunguzia Malipo yake lakini hutokosa kabisa.

Hili lilikuwa jepesi kwao kuliko lile la kwanza, kwa sababu mwenye kujiepusha na jambo hilo ameipunguzia Sala yake, lakini hakuikosa Yote.' *(Sunan At Tirmidhii)*

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuamrisha Mtu huyo arudie Sala yake kwa sababu ilibatilika kwa kukosekana *Tmaininah* - utulivu ndani yake.*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alirudia maneno hayo mara tatu ili mtu huyo apate kufaham na kua katika Sala zake zote afanye hivyo. Ambapo kuhusiana na mda wa *Tmaaninah* katika Sala basi Wanazuoni wametofautiana Juu yake.

Kwani Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao Wanasema kua *Tmaaninah* hua na ukubwa wa Kusema *Subhanah Allah.*

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao Wanasema kua *Tmaaninah* hua na ukubwa wa Kiasi viungo husika vya mwili kutulia kwa mda mfupi.

Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii wao wanasema kua *Tmaaninah* hua ukubwa wa kiasi ya Mwenye Kusali.Kutulia hadi pale itakapowezekana kutofauyosha baina ya Hatua moja na Nyengine baina yake.

Na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Hanbal wanasema kua *Tmaaninah* hua ni kiasi ya Kuupata utulivu hata kama ikiwa ni wa mda mfupi.

Na kuna hadithi isemayo kua:

عن أبي مسعودٍ الأنصاريِّ قال: قال رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم: لا تُجزئُ صلاةٌ لا يُقيمُ الرَّجُلُ فيها صُلْبَه في الرُّكوعِ والسُّجودِ

Amesema Abu Masud Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Haijuzu Sala ya yule ambae asienyoosha mgongo wake katika kurukuu kwakwe na kusujudu kwake'*(Imam At Tirmidhi)***

Na amesema Imam Ibn Arabi Al Maliki katika Ahkami Al Qur'an kua:

روى الأئمة مالك وغيره عن أنس أن النبي ﷺ قال : ''تلك صلاة المنافقين. تلك صلاة المنافقين تلك صلاة المنافقين . يجلس أحدهم حتى إذا اصفرت الشمسن وكانت بين قرني الشيطان، أو على قرني الشيطان، قام ينقر أربعا لا يذكر الله فيها إلا قليلا''. فذمها –ﷺ– بقلة ذكر الله سبحانه فيها؛ لأنه يراها أثقل عليه من الجبل، فيطلب الخلاص منها بظاهر من القول والعمل، وأقل ما يجزئ فيها من الذكر فرضا الفاتحة.

Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik na wengineo wanasema kua: 'Kutoka kwa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hio hua ni Sala ya Mnafiq, Hio hua ni Sala ya Mnafiq, ambayo mmtu hua nakaa hadi pale Jua litakapokua limeshakua na Rangi ya Njano na liko baina ya Pembe za Shaytani au juu ya Pembe za Shaytani, na kisha Mtu huyo husimama na kudonoa mara nne bila ya kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake isipokua kidogo tu'

Hivyo *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* amelaani Sala ya aina hio isiokua na utulivu ndani yake kwa sababu ndaniyake hua hakumbukwi *Allah Subhanah wa Ta'ala* isipokua kidogo tu, na hii ni kwa sababu Mtu husika hua anahisi uzito mkubwa sana juu ya Sala hio, hivyo huani mwenye kutafuta wepesi wake Ibada hio kupitia katika maneno matupu na vitendo vitupu, na kitu cha mwisho ambacho hutosheleza ndani yake kutoka katika kile kilichoFardhi katika Sala hua ni Surat Al Fatiha.''

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal katika Musnad yake kua:

عن أبي هريرة قال : قال رسول الله ﷺ : ''لا ينظر الله إلى صلاة رجل لا يقيم صلبه بين ركوعه وسجوده.

Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* haiangalii Sala ya Mtu asienyoosha Mgongo wake katika Kurukuu kwake na Kusujudu kwake.''

Hivyo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Tmaaniinah - Utulivu hua ni Wajibu katika Kurukuu na hio ni bila ya Kutokukubaliana na hii ni kulingana na Hadith ya Yule Mtu aliesali vibaya. Ama kuhusiana na Mda wa Kukaa katika hali ya Utulivu hua ni hadi pale Mtu anaesali atakapokua ametulia katika viungo vyake vyote vya mwili katika Kurukuu kwake. Na hivyo Hatua yake ya Kurukuu kua ni yenye kujiyofautisha na Kunyanyuka kwake kutoka kwenye Rukuu, hata kama ikiwa atakua amekaa katika mda zaidi ndani ya Rukuu hio kama ilivyoonesha hadith ya Mtu aliesali vibaya.**

Hivyo kama mtu atazidisha kuinama kwake na kisha akanyanyuka na Hatua hizo zikaaa zimeshikamana bila kutulia basi Mtu huyo hua hapati utulivu,na kuzidisha kuinama hua hakuchukui nafasi ya Utulivu.'

Kwa maana hio basi Wanazuoni wanakubaliana kua Tmaaninah hua hakumaanishi kukaa katika hatua moja ya Sala kwa Mda mrefu bali humaanisha Kukaa na kuhakikisha Viungo vya mwili vimetulia katika kila sehemu yake mwilini.

Na hivyokua ni vyenye kunyooka katika wakati kunyanyuka kutoka kwenye Rukuu na kukaa sawia katika wakati wa Kukaa kitako, na bila ya shaka wingi wa Dhikr Allah hutosheleza kwa mtu kua ni mwenye kuupata Utulovu katika hatua husika.'

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi basi yeye anasema kua: '**Mtu anaesali hua anatakiwa kua na Utulivu katika Kuruu kwake.'**

Yaani anatakiwa atulie kidogo anapokua katika hali ya Kurukuu,na huu ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii kama alivyosema. Ingawa kwa mtizamo wa Abu Hanifa ni kua: Tmaaninah sio miongoni mwa Fardh za Sala na hii ni kutokana na Kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema katika Qur'an kua:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱرۡكَعُواْ وَٱسۡجُدُواْ وَٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمۡ وَٱفۡعَلُواْ ٱلۡخَيۡرَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo irkaAAoo waosjudoo waoAAbudoo rabbakum waifAAaloo alkhayra laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Hajj 22:77)*

Tafsir: ***Enyi Wale ambao Mlioamini Rukuuni na Sujuduni Na muabuduni Mola wenu Na Fanyeni Mambo ya Kheri Ili Mpate kua ni wenye Kufuzu****.*

Ambapo katika aya hii *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakutaja Tmaaninah,na bila ya shaka ili Amrisho lolote la Kutekeleza kitu basi hua kinatakiwa kua ni lenye kujitosheleza.

Ambapo kwa Upande wa Al Faqif Al Mardawi Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Kuna Mitizamo miwili juu ya Hili,kuna mtizamo usemao kua Utulivu unatakiwa kiasi ya Kufanya Dhikr Allah na kuna usemao kua inatakiwa Kutulia Kidogo.'**

Ambapo manufaa ya Mitizamo miwili hii ni kua, kama mtu akisahau kufanya dhikr katika Rukuu yake au Sujud yake, au kumtukuza *Allah Subhanahwa Ta'ala* katika Kunyanyuka kwake, au kufanya Istighfar katika kukaa kwake, au kwa kutojua Lugha au kwa makusudi, basi sisi tunasema kua ni Sunnah na kama akiwa amepata utulivu ndani yake basi Sala yake hua Sahih, kulingana na mtizamo mmoja na si sahih kulingana na Mtizamo mwengine, ambapo Mahanafi wao wamesema kua Utulivu hutosheleza kaa kupatikana kutulia kwa viungo katika mda wa Dhikr Allah.'

Na amesema Ala Ad Din Abu Bakr Ibn Masud Al Kasani Al Hanafi kua: **'Tmaninah ni miongoni mwa nguzo za Sala ambayo inatakiwa kusimamiwa ndani ya Rukuu na Sujudu pia na huu ndo Mtizamo wa Imam Abu Hanifa, ambapo kw aupande wa Imam Abu Yusufbasi yeye amesema kua Utulivu unaotakiwa ni kuausuipungue kiasi yam da wa mtu kua ni mwenye kuweza kufanya Tasbih na huo ndio pia mtizamo wa Imam Al Shafii, hivyo kama mtu akikosa Utulivu ndani ya Sala' basi Sala yake hua ni Sahih kulingana na mtizamo wa Abu Hanifa na Muhammad Ash Shaybani lakini hua ni baitili kulingana na mtizamo wa Abu Yusuf na Al Shafii.**

Kama tunavyoona kua mara kadhaa katika kufafanua kwao Wanazuoni basi kua hua wanagusia Utulivu katika *Rukuu, Itidal, Sujud na Jalasa bayna Sijatayn* (Kukaa kitako baina ya Sijda mbili) mbali ya kua *Tmaaninah* hua inatakiwa katika Sala nzima.

Hivyo basi Wanazuoni hua wanatilia mkazo zaidi kuhusiana na *Tmaaninah* katika Rukuu na Sujud, kwa sababu hivyo ndivyo alivyofanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.Na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifanya hivyo kwa sababu katika Ibada ya Sala basi ni katika hatua mbili hizi za Rukuu na Sujud ndio Hatua ambazo zinazijionesha Dhahiri katika kubadilika kwake kutoka hatua moja kuingia hatua nyengine kiasi ya kua Mtu hua hawezi Kuficha haraka zake naKukosekana Utulivu ndani yake hatua hizo kivitendo.

Kwani ukitaka kumjua Mtu haraka zake katika Sala na ukamilifu wake katika Sala basi angalia Rukuu zake na Sujud zake tu, yaani hua anadonoa donoa, kutokana na uharaka wa muonekano wa vitendo vyake hivyo ndani ya Sala yake hio.

Na ndio maana ikawa kuna Hadith Tatu tofauti zinazoonya kuhusiana na Haraka katika Rukuu na Sujud, kiasi ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amefikia Kulaani Sala ya Mtu asiekamilisha Rukuu na Sujud zake. Hivyo *Tmaaninah* hua ni kuutafuta Utulivu katika Kila hatua ya Sala.

Ambapo hapa nataka tufahamiane kua *Tmaaninah* hua ni Tofauti na Khushuu ambayo humaanisha Utulivu uliojaa Ucha Mungu ndani yake.Kwani Khushuu hua inajumuisha Utulivu wa Kiroho, Kinafsi na Kimwili, na *Tmaaninah* hua ni Utulivu wa Kimwili katika Viungo vyako kua vitulie sawia katika kila hatua ya Sala kabla kuingia kwenye Hatua nyengine ya Sala.

Kwani kutokana na kua Kila Mtu anaesali hua anatakiwa asimamie *Tmaaninah* ya Sala yake mwenyewe, iwe Mtu huyo awe anasali peke yake, iwe ni Maamuma au Imam.

Hivyo anasema Imam As Suwayfi Al Shafii kua: '**Mtu anaesali hua anawajibika kulipa kila hatua ya Sala ambayo hakuipatia *Tmaaninah* ndani yake. Iwe Mtu huyo ni Imam au anasali peke yake.**

Ambapo kama Mtu huyo atakua ni Maamuma na kisha akaikosa Tmaaninah katika moja kati ya Hatua ya Sala yake, basi Mtu huyo hua anatakiwa kuendelea Kumfuata Imam katika Sala yake, na kisha pale Imam atakapomaliza Sala na Kutoa Salam,basi Maamuma huyo aliekosa *Tmaaninah* katika Rakaa yake anatakiwa asimame kisha aendelee kuisali Rakaa moja hio iliyokosa *Tmaaninah* ndani yake'

Na akasema Imam An Nafrawi Al Maliki kua: '**Imam hua habebi Jukumu lolote lile juu ya Watu anaowaongoza katika Sala zao kuhusiana na Rukuu zao, au Sujudu zao au Tmaaninah zao ndani ya Sala Husika Au kutamka *Takbirat Al Ihram* n.k.Kwani Jukumu analobeba Imam kwa ajili ya Maamuma anaowasalisha hua ni kuhusiana na yale yanayohusiana kuleta *Sijdat Sahw* kutokana na kuyasahau yeye mwenyewe anaeongoza.'**

Kwa maana hio basi Kama Maamuma atakua ni mwenye kukosa Utulivu ndani ya Sala yake, basi kosa hilo hua ni lake yeye na hua halimhusu Imam wake.Hivyo Imam hawezi kubeba Jukumu la kasoro zozote za Ndani ya Sala za Maamuma wake ikiwemo *Tmaaninah* ya Maamuma wake iwe mmoja au zaidi, kwani yeye hua anabeba Jukumu la kasoro yake na *Tmaaninah* ya Sala yake tu, na hii ni kwa sababu akikosea yeye basi na nyinyi Nyote hua mmeshakosea.

Na jukumu la kurekebisha hua ni lenu nyote kuanzia kwake yeye kisha nyote mnaemfuata.Na kama hakurekebisha kwa makusudi basi dhima anabeba yeye juu ya wote wanaomfuata, ila kama kasahau basi hua ni wajibu kukimhushana nakurekebisha.Lakini ukikosea wewe Maamuma basi umekosea wewe peke yako na jukumu la kurekebisha hua ni lako wewe peke yako na dhima hio utabeba wewe peke yako.

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi basi yeye anasema kua: '**Kama Mtu atakua anasalishwa yaani ni Maamuma, na kisha akasahau kitu ndani ya Sala, basi kulingana na Mtizamo sahih wa Wanazuoni basi ni kua, haina haja kwake kuleta Sijdat Sahw kwa sababu Imam hua anabeba jukumu la Maamuma, isipokua pale inapokua Maamuma anapokua amesahau au amekosea katika Nguzo ya Sala.'**

SUNNAN AB'AADH

❖❖❖❖

Alhamd lillah tumemalizana na Nguzo za Sala ambazo ziko 14 nazo ni:

1-Kutia Nia.
2-Kutamka Takbirat Al Ihram.
3-Qiyyam – Kusimama.
4-Qiraat Surat Al Fatiha.
5-Ruquu.
6-I'tidAl Kusimama baada ya Kurukuu.
7-Sujud.
8-Kukaa Kitako Baina ya Mbili.
9-Kutulia baina ya Sijda Mbili.
10-Tashahhud.
11-Kukaa Kitako katika Tahiyyat ya Mwisho.
12-Taslim.
13-Tartib - Kufuatisha Utaratibu huu.
14-Tmaaninah - Kua Na Utulivu ndani ya Kila Nguzo za Sala

Kwani baada ya kuangalia na kifahamishana Nguzo hizo 14 za Sala basi inabidi tufahamishane kuhusiana na Sunnah za Ndani ya Sala, Ambazo ziko za Aina Mbili nazo ni:

1-Sunnan Ab'aadh.

2-Sunnan Haiat.

Na hivyo kabla kuingia kwenye Sunnan Haiat basi kwanza tunaanza na *Sunnan Ab'aadh.*Ambapo neno Ab'adh kwa Lugha ya Kiarabu hua ni lenye kutokana na neno Ba'dha ambalo humaanisha Sehemu, Nusu au Kiini.

Ambapo Sunnah za Sala zijulikanazo kama Sunnan *Ba'adh* hua ni Sunna ambazo zinajumuisha Nusu ya sehemu ya Sala.Na kutokana na kua Sunnah hizo ni Nusu ya Sehemu ya Sala au Kiini cha Sala basi mbali ya kua ni Sunnah lakini Sunnah hizi zimekua zinamiliki Sifa ya kua ni Wajib.
Yaani ni Sunnah za Wajib ndani ya Sala.

Na kabla ya kuendelea basi tuwekeane wazi kuhusiana na mitizamo ya Wanazuoni juu ya maana na tofauti baina ya Wajib na Fardhi . na kwa Jibu la haraka na Jepesi basi tunaona kua **Fardhi hua inamaanisha Kitu au Jambo ambalo ni Lazima Kutekelezwa na hivyo tunapozungumzia Kiibada basi Usipofanya hua Unakufuru.**

Na Wajib humaanisha Kitu au Jambo ambalo hua ni Muhimu Kufanywa, lakini usipofanya hua Hukufuru bali hua unafanya Makosa badala yake na kua ni Fasiq yaani mwenye Kupenda Dhambi Waziwazi.

Ambapo anasema Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali katika Al Mustasfa fi Ilm Al Usul kua: '**Neno Wajib kwa kilugha humaanisha Kuanguka Ardhini, na Ki Tawhid humaanisha Ulazima wa Kuwepo kwa Muumba(Wajib Al Wujud).**

Na Kifiqh Neno Wajib hua ni Jambo ambalo Mtu hua atalipwa kwa kulifanya na ataadhibiwa kwa kulidharau. **Hivyo Jambo la Wajib hua halitakiwi Kudharauliwa, kwani Kulidharau kwake hua ni Kufanya makosa ya Uasi.'**

Hujjat Ul Islam Imam Abu Hamid Al Ghazali anaendelea kusema kua: '**Hivyo Hukmu ya Kitu kua Wajib hua ni sawa na kua ni Lazima na hivyo kua ni Faridha**. **Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua Fardhi hua ni Ulazima unaosimamia kwenye Uthibitisho wenye Kua na Nguvu, wenye Uhakika na Ulio Sahih**. **Na Wajibu hua ni Ulazima wa Kitu ambacho Uthibitisho wake hua hauna Nguvu sana.'***(Al Mustasfa Fi Ulum Al Usul)*

Kwani anasema pia Imam Abu Ishaq Ibrahim Ibn Ali as-Shirazi Al Shafii kua: '**Wajib na Fardhi hua ni Kitu chenye maana moja, ambacho Kukiacha kwake kitu hicho hua ni kwenye kumpelekea Mtu husika kua ni mwenye Makosa na kuadhibwa na Mola wake.'**

Na akasema Sayf Al Din Ali Ibn Muhammad Al Amidi pia kua: **'Kulingana na Wenzetu wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao Waneema kua hakuna tofauti baina ya Fardh na Wajib Lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao hua Wanaielezea Fardhi kua ni kile kilicho Lazima kwa kuthibitishwa kwa Ushahidi ulio waz**i.

Na Wajib hua ni kile kilicholazima kwa kuthibitishwa kwa ushahidi ambao hauko wazi. **Hivyo Mtizamo Sahih ni kama ilivyosema na As-habu wetu wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua:Utofauti katika Kuthibitisha Hukmu kulingana na msingi ambao hupelekea Hukmu husika kua ni yenye Kusihi ama la hua haumaanishi kua kuna utofauti wa Utekelezwaji wa Hukmu husika.'***(Al Ahkam Fi Usul Al Ahkam)*

Na imesemwa kwenye *Quwati Al Adillah fi Usul* kua: '**Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi ni kua:Kile kilicho Wajib hua kinathibitishwa kua ni Lazima kutokana na Msingi wa Uthibitisho wake kulingana na Tafsir.Kwa Mfano Salat Al Witr na Kuchinja *Udhhiya* kwa Mtizamo wao. Na Fardh hua nia kile kilichothibitishwa kwa Msingi wa Virhibitisho vilivyowazi kama vile Kusali Sala Tano, Kutoa Zakkah n.k.**

Lakini hii hua si Sahih kwa sababu Maneno haya ya Wajib na Fardhi huweza kufahamika kulingana na maana ya msingi wa Sharia, maana ya Kilugha, maana ya Matumizi ya Kawaida n.kAmbapo hua hakuna utofauti katika Matumizi yake baina ya Vilivyothibitishwa kwa Uthibitisho wa Wazi na vilivyothibitishwa kwa Uthibitisho unaotegemeana na Utofauti wa Kitafsiri.'

Hivyo Sunnan Ab'aadh ambazo ni Sunnah za Wajib za Sala hua ni Sunnah ambazo kamazinavyojielezea kimaana kua ni Sunnah zinazotiliwa Mkazo kutekelezwa ndani ya Sala.Ambapo hata hivyo Sunnah hizi sizipotekelezwa basi hakutoipelekea Sala ya Mtu husika kua ni Batili na wala haitomhitajia Mtu husika Kurudia Rakaa husika kwa sababu ya kukosekana Sunnah husika, kama vile inavyotakiwa kurudiwa Rakaa husika kutokana na Kukosekana Kwa Nguzo ya Rakaa husika au kurudiwa kwa Sala Nzima.

Bali kukosekana kwa utekelezwaji wa Sunnah Ab'aadh iwe kwa Makusudi, kwa kusahau au kughafilika huifanya Sala husika kua ni yenye Kasoro.Ambapo Kasoro hio ya Kutotekeleza Sunnah Ab'aadh yaani Sunnah ya Wajib hua ni yenye Kurekebishika kwa Kuleta Sijdat Sahw mwishoni mwa Sala husika.

Na pia hapo hapo tunakumbushana kua kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Sijdat Sahw hua ni Sunnah pia.Na kutokana na Kua ni Sunnah basi hata kama mtu akiwa hakuleta Sijdat Sahw kwa makusudi, kwa kusahau au kwa kughafilika kutokana na kuacha Sunnah ya Wajib ndani ya Sala kwa makusudi, kwa kusahau au kughafilika pia basi Sala ya mtu husika hua ni yenye kukubalika.

Na Mtu husika hua hana Makosa,lakini hata hivyo Sala husika hua si Sala kamilifu mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*Na hivyo hua ni Sala yenye upungufu wa Malipo, kwa sababu Mtu husika hua hajatekeleza Ibada yake hio ipasavyo.

Na ndio maana *Mujaddid Ad Din Hujjat ul Islami* Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali akasema kua Jambo ambalo ni la Wajib basi hua haifai kudharauliwa.

Na Tunapozungumzia kuhusiana na Sunnah za Wajib ndani ya Sala kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hua tunazungumzia Vitendo vya Aina 7 vya Sala ambavyo ni:

1-Kikao cha Tahiyyat ya Mwanzo kwa Sala yenye Tahiyyat zaidi ya Moja.

2-Kisomo cha Tahiyyat ya Mwanzo.

3-Salat Nabii Katika Tahiyyat ya Mwanzo.

4-Tashshahud - Kutoa Shahada katika Tahiyyat ya Mwanzo.

5-Kusimama katika Wakati wa Kisomo Qunut katika Sala ya Alfajir kwa kila siku na Sala ya Witr katika Nusu ya Mwisho ya Mwezi wa Ramadhan.

6-Kusoma Qunut katika Sala ya Alfajir ya Kila Siku na katika Sala ya Witr katika Nusu ya pili ya Mwezi wa Ramadhan.

7-Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na familia yake na Masahaba zake *Radhi Alahu Anhum* baada ya kisomo cha Dua ya Qunut.*(Safinat An Naja)*

Hivyo hizi ndio Sunnah za Wajb ambazo Mtu akiwacha kutekeleza moja wapo au zaid kati yao basi humbidi kuleta Sijda Sahw kufidia mwishoni mwa Sala yake**.**

Kwani Ingawa Sunnan Ab'aadh hua haziifanyi Sala kua ni yenye kubatilika kutokana na kutotekelezwa kwake, lakini hata hivyo Sunnah hizi hua zinatakiwa kutekelezwa na Mtu anaesali. Hata kama Mtu huyo atakua ni mwenye Kusali Qadhaa Salat yaani Sala ya Kufidia au kulipa. Na kwa maana hio basi kama mtu akiwa hakutekeleza Sunnah hizi za Wajibndani ya Sala za Qadhaa basi hua pia ni Wajib wake kuleta Sijdat Sahw kwani Sala husika hua na Kasoro.

Na Ingawa kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua ni wenye kutilia mkazo Kusali Sala ambayo haijasalisa hapo hapo Mtu utakapokumbuka, au Utakapoweza. Lakini hata Hivyo *Mujaddid Ad Din* Imam Abd Allah Alawi Al Haddad Al Shafii ambae ni mwanzilishi wa Tariqa Alawiyyah basi yeye anasema kua: **'Mtu hua anaruhusika Kusali Salat Qadhaa kwa Kadri atakavyoweza, hivyo kama ikiwa Mtu ana madeni mengi ya Sala basi bila ya Shaka Mtu husika hua anaweza kupunguza Madeni hayo kwa kadri awezavyo na kwa utulivu zaidi.'**

Na akasema Imam Ad Dasuqi Al Hanbali kua: **'Wajibu wa kulipa Sala hua ni wa kati na kati, na hivyo hua inaruhusika kusali Sala za Qadha za Siku mbili au zaidi ndani ya Siku moja, kwani hua haitoshelezi kulipia Sala za Siku moja tu, labda pale itakapokua Mtu husika ni mwenye khofu ya kutoweza kuwahudumia watu wa familia yake, kama atakua ni mwenye kusali Qadhaa Salat za zaidi ya Siku moja ndani ya Siku moja.'**

Kwani amesema Abd Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Katika Vita vya Khandaq Makafiri walituzuia pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutokana na kusali Sala ya Al Asr hadi Jua lilipokua Jekundu. Hivyo R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Wametushughulisha sisi hawa katika wakati wa Sala ya Al Asr, Allah aijaze Miili yao na Makaburi yao kwa Moto.'**

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua:**'Kuna Makubaliano ya Wanazuoni ambao Mtizamo wao ni wenye Kukubalika, ambao ni wenye kusema kua: 'Yeyote Mwenye Kuiacha Sala kwa Makusudi basi hua ni Wajibu kwake kuilipa Sala hio'***(Al Majmuu)*

Ama kuhusiana na uthibitisho wa Tahiyyat ya kwanza kua ni Sunnan Ab'aadh na hivyo mtu akiiwacha humbidi kulete Salat Sahw basi ni ile haditi isemayo:

عَنْ عَبْدِ اَللَّهِ بْنِ بُحَيْنَةَ –رَضِيَ اَللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ– { أَنَّ اَلنَّبِيَّ – صلى الله عليه وسلم –صَلَّى بِهِمُ الظُّهْرَ , فَقَامَ فِي اَلرَّكْعَتَيْنِ اَلْأُولَيَيْنِ , وَلَمْ يَجْلِسْ , فَقَامَ اَلنَّاسُ مَعَهُ , حَتَّى إِذَا قَضَى اَلصَّلَاةَ , وَانْتَظَرَ اَلنَّاسُ تَسْلِيمَهُ , كَبَّرَ وَهُوَ جَالِسٌ . وَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ , قَبْلَ أَنْ يُسَلِّمَ , ثُمَّ سَلَّمَ }

Kutoka Abd Allah Ibn Malik Ibn Buhainah *Radhi Allahu Anhu kua:Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha sisi Salat Al Dhuhr, na hakukaa kitako baada ya Sujud ya Mwisho ya Rakaa ya pili na watu wakasimama pamoja nae. Na hivyo alipomaliza kusali, na watu wakategemea kua atatoa Salam, basi akatamka Takbir na kisha akasjudu Sijda mbili kabla ya Kutoa SalamNa kisha akanyanyua Kichwa na akatoa Salam.'*(Sahih Bukhari)***

Naam..hii ni Hadith ambayo inatoa Hukm yenye Kuthibitisha Umuhimu wa Kutekelrleza Tahiyyat ya Kwanza ndani ya Sala ambayo hua ni Sunnah Ab'aadh au Sunnah ya Wajib na ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoisahau au alipoiwacha na kisha akakumbuka basi alileta Sijdat Al Sahw kufidia kasoro hio ya kutosoma Tahiyyat ya Kwanza ya Sala.

Na kama tunavyojua kuhusiana na Udhaifu wa Ibn Adam kimaumbile, kwani mbali ya kua Sala hua ni Ibada ya Kiroho,Kimoyo na Kimwili.Ambayo humpelekea Ibn Adam kua ni mwenye kusimama mbele ya Mola wake huku akiwa ni mwenye Kumtukuza kwa Unyenyekevu.

Lakini Ibn Adam ni Kiumbe aliumbwa na hisia za Usahaulivu, ambazo hua ni kwa ajili ya Manufaa yake.Kwani hisia za Ushaulivu humsaidia Ibn Adam kusahau Huzuni, Matatizo na Misiba anayokutana nayo katika Maisha. Kwani akiwa hayasahau matukio hayo basi Ibm Adam hatokua na uwezo wa kufanya kitu chochote bali atakua kama mwenda wazimu.

Na Kimaumbile hapa Duniani basi kwa kila chenye faida hua kina hasara zake, ambapo hasara ya Hisia za Sahau hua ni pale Ibn Adam anapokua ni Kumsahau Mola wake, jambo ambalo humpelekea Kuingia katika Maangamizo. Hivyo Kutokana na kua na sifa ya Kusahau basi Ibn Adam huweza pia kusahau ndani ya Ibada yake ya Sala, na hivyo akawa ni mwenye kuongeza ama kupunguza baadhi ya mambo ndani ya Sala yake.

Na hivyo humbidi kulipia ili kufidia alichokipunguza ndani ya Sala yake hususan kile kilichosahauliwa kinapokua ni miongoni mwa yaliyo Wajib kama Sunnah Ab'aadh na hivyo Hadith inatuonesha namna ya Kufidia kasoro hio kupitia kwenye mfano wa namna alivyofanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kuleta Sijdat Sahw baada ya Tahiyyat ya pili kabla ya kutoa Salam.

Ambapo tukio hili la kusahau kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* halimaanishi kumshusha yeye Darja bali ni lenye kumaanisha Kutoa mafunzo kwetu sisi mimi na wewe kuhusiana na Umuhimu wa Kutekeleza Ibada ya Sala kwa mpangilio wake, na kutuonesha nini cha kufanya pale tutakapokosea.

Na kwa upande mwengine basi kuhusiana na Salat An Nabii kua ni Sunnah Ab'aadh tunayaona haya katika Hadith ya Shu'bat tuliyoiangalia hapo kabla isemayo:

حَدَّثَنَا مَحْمُودُ بْنُ غَيْلاَنَ، حَدَّثَنَا أَبُو دَاوُدَ، - هُوَ الطَّيَالِسِيُّ حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، أَخْبَرَنَا سَعْدُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، قَالَ سَمِعْتُ أَبَا عُبَيْدَةَ بْنَ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مَسْعُودٍ، يُحَدِّثُ عَنْ أَبِيهِ، قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم إِذَا جَلَسَ فِي الرَّكْعَتَيْنِ الأُولَيَيْنِ كَأَنَّهُ عَلَى الرَّضْفِ .

Amesema Muhammad Ibn Ghaylani, kua amesemaa Abu Daud ambae ni At Tayalisi kua amesema Shu'bat kua amesema Said Ibn Ibrahim kua nimemsikia mimi Abu Ubaydah Ibn Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akikaa kwenye Rakaa mbili za Kwanza (Kwenye Tahiyyat ya kwanza) ilikua kama Mtu aliekaa kwenye Mawe ya Moto.'*(****Sunan At Tirmidhii, Imam Abu Daud, Imam An Nasai,Al Majmuu Imam An Nawawi)*

Ambapo kutokana na Hadith hii Wanazuoni wanasema kua Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kulingana na Hadith hii basi tunaona kua Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya Pili hua ni Fardhi na katika Tahiyyat ya Mwanzo hua ni Sunnah'***(Al Majmuu)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Khatib Al Shirbini basi yeye anasema kua: '**Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat inayofuatiwa na Taslim hua ni Fardhi hata kama Sala husika itakua haina Tahiyyat ya kwanza kama Sala ya Al Fajr kwa mfano**. **Lakini Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni ni kua Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya kwanza basi hua ni Sunnah Lakini hata hivyo Mtizamo Sahih miongoni mwa Wanazuoni kuhusiana na kuitumia Salam Familia ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya mwanzo hua si Sunnah kama ilivyoonesha Hadith iliyotajwa hapo kabla.'***(****Al Mughni)*

Kwani kwa upande mwengine basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao Wanasema kua: '***Kumsalia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya mwanzo hua ni Sunnat Ab'aadh kwa sababu hua ni Wajib kwani ni Wajib Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kila linapokua Linatajwa jina lake, na hivyo katika Tahiyyat ya Kwanza hua hakuna Ulazima wa Kuisalimia Familia ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***(*Hashiyyah Imam Sulayman Al Bujaraimi Al Shafii)*

Kwani anasema Mujaddid Ad Din Mujtahid Imam Al Madhhab Imam Muhammad Idtis Al Shafii kua: **Kushuhudia na Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya Mwanzo ya kila Sala yenye Tahiyyat mbili, isipokua Salat Al Fajr Hivyo kama Mtu akiwa hakushuhudia wala hakumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat yake ya Mwanzo kwa kusahau, basi haimhitajii Mtu huyo kuirudia Sala yake bali Itamhitajia Mtu huyo kuleta Sijdat Sahw.'***(Kitab Al Umm)*

Ambapo Mtizamo hui wa Imam Al Shafii ambao ndio wa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na ndio pia Mtizamo wa Imam Abd Rahman Al Shaabi, Imam Ibn Hazim Al Andalus, Imam Al Ajuri na Imam Ibn Hubayra.

Na kwa upande wa Imam Ibrahim An Nakhai na Imam Sufyan Ath Thary basi wao wanasema kua: '**Hakuna ulazima kwa Mwenye Kusali kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya Mwanzo.'**

Ambapo Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Malik, na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na ndio uliokua Mtizamo wa zamani wa Imam Al Shafii katika Kitabu cha Al Risala, kabla ya kuhamia Misri na kuandika Kitabu cha Al Umm.

Kwani aliulizwa Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua: '**Kama Mtu akisahau na kisha akasoma Tahiyyat ya kwanza na kisha akasoma pia Salat Ibrahimiya Ndani yake,afanyeje.'**

Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi akasema: **'Kama ikitokezwa kua Mtu ametamka Dhikr Sio kwenye sehemu yake, au akasoma Qur'an ndani ya Ruquu au ndani ya Sujud, au akasoma Tahiyyat wakati akiwa yuko kwenye Kisimamo, au akisoma Salawat Ibrahimiyyah kwenye Tahiyyat ya kwanza, au akasoma na Sura nyengine baada ya Surat Al Fatiha katika Rakaa ya tatu na ya nne ya Sala, n.k kutokana na kusahau, basi kuna Mitizamo miwili juu yake.**

Ambapo Mtizamo wa kwanza ni kua: 'Haihitajiki kwake Mtu huyo Kuleta Sijdat Sahw, na hii ni kwa sababu kuyafanya mambo hayo hua hakubatilishi Sala ya Mtu husika hata kama ni kwa makusudi, hivyo haina haja kwa mtu kuleta Sijdat Sahw kama ikwa amefanya hivyo ksa kusahau, kwani hua ni sawa na kutofanya kitu cha Sunna ndani ya Sala.'

'Na Mtizamo wa pili ni kua Mtu huyo aliefanya hivyo hua anawajibika kuleta Sijdat As Sahw na hii ni kutokana na Uthibitisho wa Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*aliposema:**Kama ikiwa mmoja wenu atasahau kitu ndani ya Sala basi na afanye Sijdat As Sahw*(Sahih Muslim)***

Hivyo basi kama tukisema kua mtu huyo atatakiwa Kuleta Sijda Sahw basi hii hua ni kutokana na pendekezo na wala si Lazima, kwa sababu kurekebisha kitu ambacho hakina Ulazima hua hakuna Ulazima.'

QUNUT – KATIKA SALATAL FAJIR.

❖❖❖

Neno Qanata kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kujitolea, Kua Mtiifu, Kua na Ikhlasi katika Kitu, Kusimama kwa Roho, Mwili na Moyo wote kwa mda mrefu na Unyenyekevu ndani ya Ibada ya Sala.

Ambapo amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* Kua:

عن جابر رضي الله عنه قال: قيل للنبي صلى الله عليه وسلم: أيُّ الصلاة أفضل ؟ قال : طول القنوت

'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*aliulizwa:** '**Sala Bora ni ipi?' Ambapo nae akasema:'Tuul Al Qunut (Kisimamo Kiref**u)'*(Sahih Muslim)*

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kuhusiana na maneno ya Hadith hii kua: '**Kulicho kusudiwa hapa - *Tuul Al Qunut* - katika Hadith hii ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni basi ni Kisimamo Kirefu Cha Sala.'**

Neno *Qanata* ndio lililotoa neno Qunut ambalo hua kinamaanisha Jina la Dua inayoombwa Ndani ya Sala katika wakati ambao Mtu anaesoma hua amesimama ndani ya Sala.

Na hivyo anasema Imam Al Azhari kua: **'Maana ya Qunut Katika Sala ya Alfajir hua ni Kisomo cha Dua mara baada ya Kurukuu kutoka katika Rakaa ya Mwisho ya Sala.'**

Na pia Qunut kimaana basi hua ni Kua na Utiifu Mkubwa Sana uliojaa ukimya kama isemavyo Hadith isemayo:

حَدَّثَنَا أَحْمَدُ بْنُ مَنِيعٍ، حَدَّثَنَا هُشَيْمٌ، أَخْبَرَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ أَبِي خَالِدٍ، عَنِ الْحَارِثِ بْنِ شُبَيْلٍ، عَنْ أَبِي عَمْرٍو الشَّيْبَانِيِّ، عَنْ زَيْدِ بْنِ أَرْقَمَ، قَالَ كُنَّا نَتَكَلَّمُ خَلْفَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فِي الصَّلاَةِ يُكَلِّمُ الرَّجُلُ مِنَّا صَاحِبَهُ إِلَى جَنْبِهِ حَتَّى نَزَلَتْ

Amesema Ahmad Ibn Mani'I kua amesema Hushaym kua amesema Ismail Ibn Abi Khalid kua amesema Harith Ibn Shubayl kua amesema Amr Al Shaybani kua amesema Zaid Ibn Arqam *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Sisi tulikua tukizungumza Nyuma ya *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*wakati tukiwa ndani ya Sala, ambapo mmoja miongoni mwetu alikua akizungumza na mwenzake, hadi pale iliposhushwa aya isemayo:'

﴿حَافِظُواْ عَلَى ٱلصَّلَوَاتِ وٱلصَّلَاةِ ٱلْوُسْطَىٰ وَقُومُواْ لِلَّهِ قَانِتِينَ﴾

Hafi*dh*oo AAala alssalawati waalssalati alwusta waqoomoo lillahi qaniteena*(Surat Al Baqara 2:238)*

*Tafsir: **Kuweni wenye uhifadhi Juu ya Sala Hususan Sala ya Kati kati (Ya Al mda wa Asr) Na simameni Mbele ya Allah Mkiwa katika Utiifu wa hali ya Juu kabisa uliojaa ukimya**.*

فَأُمِرْنَا بِالسُّكُوتِ وَنُهِينَا عَنِ الْكَلاَمِ

Na hivyo ikawa ni wenye kuamrishana kukaa kimya na kukakatazana Maovu. *(Jamii At Tirmidhi)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Zajjaj basi amesema kua: **'Inafahamika sana kua Kilugha kua Qunut maana yake hua ni Kisomo cha Dua'**

Na akasema Imam Ibn Arabi kua**: 'Mimi nimefuatilia Asili ya Qunut na nikaona kua ni katika hali 10 zifuatazo:'**

1 — الطاعة – **Utiifu.**

2 — العبادة — **Kuabudu.**

3 — دوام الطاعة – **Utiifu Wenye Kudumu.**

4 — الصلاة – **Sala.**

5 — القيام **Kisimamo.**

6 — طول القيام –**Kisimamo Kirefu.**

7 — الدعاء — **Dua.**

8 — الخشوع — **Khushuu.**

9 — السكوت – **Kukaa Kimya.**

10 — ترك الالتفات — **Kutogeuka huku wala kule.**

Maana zote hizi hua ni zenye kukubalika, amapo ya mwanzo hua ni Kukaa Kimya, Kua na Unyenyekevu na Kisimamo*.'(Al Aridha)*

Na kwa kua Qunut hua ni Dua inayosomwa ndani ya Kisimamo cha Sala. Basi anasema tena pia Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: '**Mtizamo uliokua Sahih ambao umelezewa wazi na kukubalika na Wengi Miongoni mwa Wanazuoni ni kua Hakuna Maneno ya Duaa Maalum ambayo inatakiwa kusomwa ndani ya Qunut bali Mtu anaweza kusoma Dua yoyote.'** *(Al Majmuu)*

Ama kuhusiana nayo Qunut basi kuna Mitizamo tofauti juu ya wakati wa Kusomwa Dua ya Qunut kwani kuna ambao husoma Dua ya Qunut kabla ya Kurukuu. Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab mengineyo basi wao hua wanasoma Qunut Baada ya Rukuu, mara tu baada ya kusema *Rabbana wa Laka Al Hamd* kabla ya Kusujudu, na kama tulivyoona hapo awali kua Qunut ni miongoni mwa *Sunnan Al Ab'aadh,* ambapo kulingana na Mtizamo wa Imam Al Shafii basi Sunnah hizo kwa ujumla ni:

1-Kikao cha Tahiyyat ya Mwanzo kwa Sala yenye Tahiyyat zaidi ya Moja.

2-Kisomo cha Tahiyyat ya Mwanzo.

3-Salat Nabii Katika Tahiyyat ya Mwanzo.

4-Tashshahud - Kutoa Shahada katika Tahiyyat ya Mwanzo.

5-Kusimama katika Wakati wa Kisomo Qunut katika Sala ya Alfajir kwa kila siku na Sala ya Witr katika Nusu ya Mwisho ya Mwezi wa Ramadhan.

6-Kusoma Qunut katika Sala ya Alfajir ya Kila Siku na katika Sala ya Witr katika Nusu ya pili ya Mwezi wa Ramadhan.

7-Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na familia yake na Masahaba zake *Radhi Alahu Anhum* baada ya kisomo cha Dua ya Qunut.*(Safinat An Naja)*

Na amesema Hasan Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alinifundisha Mimi maneno ya Kusema kwenye Qunut ya Wtir kua:**

اللَّهمَّ اهدِنِي فيمن هديت، وعافِنِي فيمن عافيتَ، وتولَّنِي فيمن تولَّيتَ، وبارِك لي فيما أعطيتَ، وقِني شرَّ ما قضيتَ، إنَّكَ تقضي ولا يقضى عليْكَ، وإنَّهُ لا يذلُّ من واليتَ، ولا يعزُّ من عاديتَ، تبارَكتَ ربَّنا وتعاليتَ

Allahuma Ihdini Fii Man Hadayt **- Ya Allah Niongoze Kama Ulivyowaongoza Waliongoka.**

Waafini Fiiman aAafayt **- Na Niokoe kama Ulivyowaokoa Waliokoka.**

Watawalani Fiiman Tawalayh **- Na Nisimamie kua miongoni mwa Uliowasimamia.**

Wabarik Fiiman A'atayt **- Na Nibariki Katika Ulichonipa.**

Waqinni Sharran Ma Qadhait **- Na Nikinge na Shari Ulizoniadikia zinifike.**

Innaka Taqdhi wala Yuqdha Aalayk **- Kwa Hakika wewe ndie Mwenye Kutaka Na Hakuna Anaeweza kutaka Dhidi yako.**

Wainnahu la Yadhilu Man Walayt **- Na kwa Hakika Hadhaliliki Yule Ulie karibu nae.**

Wala YaiI'zu Man Adayt **- Na Wala Hatukuki Alie Adui Yako.**

Tabarakta Rabbana Wa TaA'alayt **- Baraka zote ni Zako Ewe Mola wetu na Utukufu ni wako.**
(Sunan At Tirmidhii, Sunnan Abu Daud, Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal)

Naam..Hii ni moja kati ya Hadith zinazozungumzia kuhusiana na Dua Qunut ya ndani ya Sala, ya Witr na ya Sala Alfajir pia ambayo ailiifundisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Na hua inapendekezwa kwa kumalizia kwa kusema:

فَلَكَ الحَمْدُ عَلَى مَا قَضَيْتَ، نَسْتَغْفِرُكَ اللَّهُمَّ رَبَنَا وَنَتُوْبُ إِلَيْكَ، وَصَلَّى اللهُ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ النَّبِيِّ الأُمِّي وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَسَلَّمْ

Falak-Al Hamdu 'alā Mā Qadhaita, Nastaghfiruka wa Natūbu ilayk Wa Sallallāhu 'alā Sayyidinā Muhammadin Nabiyyi Al Ummīyi wa 'alā ālihi wa Sahbihi wa Salam.

Kwa hakika wewe ndie pekee mwenye kustahiki shukrani kwa unayoamua kuyafanya tunaomba Msamaha wako na tunarudi kwako kwa kutubu.

Sala zimfikie Sayyidna Muhammad *(Salallahu alayhi wa Salam)* Nabii wa Umma Usiosoma na Familia yake na Masahab zake kwa ujumla na salam.

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi kuhusiana na Neno Umm kua: **'Kusoma na Kuandikani moja kati ya mambo rahisi kabisa katika Maisha, lakini hata hivyo Elimu aliyokuja nayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salamna kuikabidhi Ulimwenguni* basi ni ktu ambacho hakijawahi kutolewa na Kiumbe aliekua hai yeyote, na hivyo hii ni miongoni mwa Miujiza kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*hakua ni mwenye kuweza kitu Rahisi lakini alikua ni mwenye uwezo wa jambo gumu zaidi '**

Na bila ya shaka kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Qunut hua ni Sunnan Ab'aadh.Ambayo Mtu asieitekeleza katika Sala ya Fardh ya Al Fajir na Katika Sala ya Sunnah ya Witr basi hutakiwa Kuleta Sijdat Sahw badala yake.Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik.

Kwani anasema Imam Muhammad Hasan Hitou Al Shafii kwenye kitabu chake cha Kashf Al Satr An Sunniyat Al Qunut Fii Al Fajr kua: '**Wanazuoni ni wenye kukubaliana kua Dua ya Qunut hua ni Dua inayosomwa katika Hali tatu zifuatazo:**

1-Qunut Katika Salat Al Fajr.

2-Qunut Katika Rakaa ya Mwisho ya Witr.

3-Qunut Katika Sala zote za Nawazil (katika Wakati wa Misiba na Mitihani ya Maangamizo)

Na kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Dua ya Qunut hua inasomwa katika hali hizo tatu katika hatua zifuatazo za Sala husika:

1-Qunut ya Salat Al Fajr hua ni Baada ya Itidal ya Rakaa ya mwisho ya Salat Al Fajr.

2-Qunut ya Salat Al Witr hua ni Baada ya Itidal ya Kila Rakaa ya Witr katika Nusu ya pili ya Mwezi wa Ramadhani.

3-Qunut Katika (Nawazil) Wakati wa Sala zote katika Wakati wa Mitihani ya Maangamizo hua ni baada ya Rukuu ya Rakaa ya Mwisho ya Sala ya Nawazil.*(Kashf Al Satr An Suniyyat Al Qunut fi Al Fajr)*

Kwani anasema Shaykh Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Hakuna kutokukubaliana katika Skuli ya Madhhab yetu kuhusiana na Qunut kua ni yenye Kupendekezwa Sana katika Itidal ya Rakaa ya mwisho ya Salat Al Fajr**. **Kwani Qunut katika Salat Al Fajr ni Sunnah Ab'aadh, ambayo atakeiwacha kwa makusudi, au kwa kusahau basi hua ni Wajibu kwake Kuleta Sijdat Sahw'***(Minhaj Talibin)*

Na akasema tena Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Sharaf An Nawawi katika *Kitab Al Adhkar* kua: '**Fahamuni kua Qunut ni Sunnah iliyothibitishwa katika Skuli ya Madhhab yetu katika Salat Al Fajr**. **Na hivyo kama Mtu akiiwacha Qunut basi Sala yake haibatiliki lakini Sala hio hua inakua na Kasoro, na hivyo Mtu husika humbidi kuleta Sijda Sahw kwa kuiwacha Qunut iwe kwa Makusudi au kwa kusahau.'***(Al Adhkar)*

Kwani amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:

مَا زَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْنُتُ فِي الْفَجْرِ حَتَّى فَارَقَ الدُّنْيَا

‘***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **kamwe hakuwahi kuwacha Kusoma Qunut katika Salat Al Fajr hadi alipoondoka Dunian**i *’(Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal,Sunan Al Bayhaqi, Mustadrak Al Hakim, Al Allamah Al Mualimi)*

Ambapo amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: ‘**Hii ni Hadith Sahih iliyonukuliwa na Wanazuoni kadhaa wa Hadith ambao Wamesema kua ni Sahih Hadith’***(Al Khulasa)*

Na anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Yazid Ibn Majah Al Rab Al Qazwini kua:

حَدَّثَنَا نَصْرُ بْنُ عَلِيٍّ الْجَهْضَمِيُّ، حَدَّثَنَا سَهْلُ بْنُ يُوسُفَ، حَدَّثَنَا حُمَيْدٌ، عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ، قَالَ سُئِلَ عَنِ الْقُنُوتِ، فِي صَلاَةِ الصُّبْحِ فَقَالَ كُنَّا نَقْنُتُ قَبْلَ الرُّكُوعِ وَبَعْدَهُ

Anasema Nasr Ibn Ali Al Jahdhami kua amesema Sahl Ibn Yusuf kua amesema Humayd kua;Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* aliulizwa kuhusiana na Qunuti katika Sala ya Asubuhi ambapo nae akasema: Sisi Tulikua tukisoma Qunut Kabla Rukuu na Baada ya Rukuu pia.’*(Sunan Ibn Majah)*

Naam..hii ni miongoni mwa Hadith zinazoelezea namna Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walivyokua wakisoma Qunut katika Sala ya Alfajir ambapo kutokana nayo hadith hii basi tunaona kua kuna kutofautiana kwa Wanazuoni kuhusiana na sehemu ya kusoma Qunut katika Salat Al Fajr. Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Abu Fadhl Shihab Ad Din Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii anasema kua: **‘Sanad ya Hadith hii ni Sahih isiyokua na Kasoro**’*(Fat-h Al Bar)*

Na hivyo basi mbali ya kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanasoma Qunut baada ya Kurukuu lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: ‘**Qunut inaweza ikasomwa Kabla au Baada ya Rukuu ya Rakaa ya Pili ya Sala ya Alfajir**. **Lakini hua ni bora zaidi kuisoma Kabla ya Kurukuu na hii ni kulingana na Mtizamo ambao ni Mashhur katika Madhhab ya Imam Malik**. **Na Qunut inatakiwa isomwe kwa Sauti ambayo mwenye kuisoma atakua ni mwenye kuisikia, na Mikono hua haitakiwi Kunyanyuliwa kama inavyonyanyuliwa na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii.’***(Imam Abi Zayd Al Qayrawani)*

Ambapo anasema Imam Abu Walid Al Baji Al Maliki kua: **‘Kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Shafii basi Qunut hua ni Wajib katika Sala ya Alfajir, ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wametofautiana kidogo na Madhhab ya Imam Al Shafii. Kwani Madhhab ya Imam Malik wao wanasema kua Qunut katika Salat Al Fajr ni Mustahab yaani inapendekezwa (tofauti na Madhhab ya Imam Al Shafii ambao wao Wanasema ni Sunna). Na kuna utofauti pia wa Njia ya Kusomwa kwake kwani Madhhab ya Imam Malik wanasoma Kabla ya Kurukuu.’**

Imam Al Baji anaendelea kusema kua: ‘**Kwa Upande wa Imam Abu Hanifa na Imam Sufyan Ath Thawry basi wao wanasema kua Qunuti hairuhusiki katika Sala yeyote ya Fardhi. Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao Wanasema kua Qunut hua inasomwa katika baadhi ya Wakati kulingana na Mazingira maalum.’**

Ambapo hapa inabidi tufahamiane kua Mtizamo huu wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal unapingana na Kisomo cha Qunut, na hii ni kwa sababu Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Hanbal umeigawa Qunut katika hali mbili tofauti kama alivyoelezea Imam Ibn Al Qayyim kua Qunut

ziko za aina mbili ambapo aina ya kwanza hua ni Dua ya aina yeyote kwa Ujumla, na aina ya pili hua ni Dua Maalum.

Kwani Imam Ibn Al Qayyim anatuambia kua:**'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut katika Wakati wa *(Ainda Al Nawazil)* Mitihani**. **Ambapo alisoma kuwaombea baadhi ya Watu ili *Allah Subhanah wa Ta'ala* awalaani, na pia alisoma baadhi ya wakati kwa ajili ya kuwaombea baadhi ya watu kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwacha Kusoma Qunut baada ya wale aliowaombea walaaniwe walipotubu na wale aliowaombea Wepesi walikua huru kutokana na Mitihani yao, Hivyo Qunut haisomwi katika Salat Al Fajr tu bali inasomwa pia hata katika Salat Al Maghrib.'***(Zadd Al Maad)***

Ambapo Imam Malik Ibn Anas anasema kua: '**Mtu anaesoma Qunut Katika Sala ya Alfajir kabla ya Kurukuu hua haina haja kwake kufanya Takbir: Na Qunut ni Nyepesi kwani unaweza kuisoma Kabla ya Kurukuu au baada ya Kurukuu, lakini Mimi mwenyewe hua nasoma Qunut kabla ya Kurukuu.Na Mtu anaesahau Kusoma Qunut basi hua haina haja kwake kuifidia.'**

Na pia hakuna Kisomo maalum cha Qunut au Mda Maalum wa Kisimamo na hakuna Tatizo kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* chochote kile ndani yake katika Sala ya Fardhi , iwe cha Kidunia au Kiakhera. **Kwani amesema Urwa Ibn Al Zubayr kua: Kwa Hakika Mimi humuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* kila kitu changu Ndani ya Sala yangu hadi Chumvi ya kupikia chakula change.'***(Tartib Al Madarik wa Taqrib Al Masalik)*

Ambapo wanasema Imam Bukhari na Imam Muslim kua: **'Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* aliulizwa:** '**Hivi Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Qunut katika Sala ya Asubuhi?'**

Ambapo nae akajibu: 'Naam'.

Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* akaulizwa tena: 'Jee ilikua ni kabla ama ni baada ya Rukuu?'

Ambapo nae akasema: 'Ni baada ya Rukuu'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Na bila ya shaka hili suali la Qunuti katika Salat Al Fajir ni miongoni mwa Mada ambayo ina mivutano mingi kwa wengi sana miongoni mwa Jamii yetu kutokana na Maradhi ya Ubinafsi na Ujinga Ndani ya Nyoyo zetu Waislam. Kwani hali imefikia kiasi ya kua kama Vile Mgonjwa anaeumwa kisha akaambiwa kua Dawa yake unatakiwa Unywe Asali kijiko kimoja kila siku Asubuhi kabla ya kula kitu chochote na Utapona. Basi Wallahi kwa hali tuliyokua nayo basi Mgonjwa huyo anakuambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakunywa Asali kijiko kimoja kila siku asubuhi,hivyo hio ni Bidaa na haifai.

Kwani Mithili ya Mgonjwa na Dozi ya Kijiko kimoja cha Asali basi ndio Tulivyosisi Waislam wa leo. **Kwani Waislam wa leo tuna Matatizo mengi sana katika Maisha yetu, ikieermo Udhaifu wa Imani, Upotovu unaosababishwa na Utandawazi, Kupungukiwa kwa Baraka katika Kipato, Katika Ardhi Mashambani, n.k.**

Na kama Tulivyoona maana ya Dua ya Qunut basi ni Kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* atupe Utatuzi wa Matatizo hayo hayo tuliyokua nayo Katika mazingira Ya Maisha yetu.

Lakini Unapomwambia Mtu kua Dua ya Qunut ndani ya Sala ya Al Fajir ndio Utatuzi wa Matatizo yetu basi yeye anakuambia kua Qunut katika Salat Al Fajr ni Bidaa na Haifai. **Hivyo**

Jee Utamfahamisha vipi Mtu kama huyo? Mgonjwa Ambae anaona kua Dawa ya Kuomba Dua ili kuondolewa Matatizo hayo na Mola wake katika Nafsi yake, Familia yake, Jamii yake n.k katika Sala ya Al Fajir kua Haifai?

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: '**Na inapendekezwa pia Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qunut**. **Pale Imam anapomtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala,* ambapo hua haitakiwi kusema Amiin bali hua inatakiwa Kutukuza.Na Dua ya Qunut ina Manufaa mengi sana na Baraka nyingi sana hususan pale inapokua Mtu husika hua ni mwenye Kuianza siku yake kwa Dua hio yenye Dhikr, Kuomba Hifadhi na kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala'***(*Al Majmuu)*

Ambapo Imam Al Shawkani Al Hanbali kua:**'Na Fahamu kua kuna Makubaliano juu ya kukubalika kutosoma Qunuti bila ya kua na sababu yeyote katika Sala ya Adh Dhuhr, Salat Al Asr,Salat Al Maghrib na Salat Al Ishaa.Ama kuhusiana na Qunut katika Salat Al Fajr basi kuna kutokukubaliana juu yake kuhusiana na Sala za Fardhi .'***(Nayl Al Awtar)*

Ambapo amesema Baraa Ibn Al Aazib *Radhi Allahu Anhu* kua:**'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Qunut katika Sala ya Al Fajr na Sala ya Magharibi pia.'***(Imam Muslim)*

Ambapo Hadith hii inadhihirisha yale yaliyokua yakifanywa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala zake, ambapo miongoni mwao ni Qunut katika Salat Al Fajr na Salat Al Maghrib.Na Hadith hii ni yenye kuelezea Vitendo vilivyo katika hali ya Muendelezo na hivyo kumaanisha Kuruhusika kwake vitendo hivyo ambavyo ni vya kisomo cha Dua ya Qunut.

Na hivyo Kitendo hicho kua ni chenye kukubalika kufuatwa kutokana na kua ni Sunnah ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Na kwa kua Hadith hii inaelezea Sala mbili za Al Fajr na Maghrib basi kuna baadhi wanaweza wakajiuliza, kwa kusema: '**Kama hali ikiwa ndio hivyo basi kwanini Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Wasisitize Qunut ya Al Fajr tu?'**

Ambapo kuhusiana na Suali hili basi anasema Imam Maahiri wa Hadith wa Kikurdi wa Madhhab ya Imam Al Shafii Abu Amr Uthman Ibn Abd Rahman Ibn Salah Al Kurdi Al Shahrzuri Al Shafii kua: '**Hua haidhuru kwetu sisi kihoja kua Wanaopinga watasema kua Qunut katika Sala ya Maghrib iliachwakwa sababu ya kua pia hakuna Qunut katika Sala ya Al Fajr**. **Na watu walifanya hivuo katika Sala ya Maghrib kwa sababu kuachana nayo Qunut ya Sala ya Magharibi hakukutazwa**. **Hivyo Walioachana na Qunut, basi hayo ndio yaliyokua Majaaliwa yao kuachana na Qunut ya Sala Moja kati ya Qunut za Sala mbili hizi Jambo ambalo halikukatazwa kiziada.'***(Sharh Al Wasit)*

Na amesema Imam Muhammad Ibn Sirin Al Basr kua: **'Mimi nilimuuliza Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema:** '**Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut katika Sala ya Al Fajir?''**

Ambapo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Naam, alifanya Qunuti baada ya Kurukuu kwa Muda mfupi.''(*Bukhari na Muslim)*

Ambapo hadith hii pia inatuonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Qunut katika Sala ya Al Fajir na hivyo basi, jambo hilo ni lenye kukubalika. Hivyo Imam Ibn Salah anaendelea kusema kua: '**Amesema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua, Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali *Radhi Allahu Anhum,*Wote walisali na Kusoma Dua ya Qunut katika Salat Al Fajr baada ya Rukuu baada ya Kufariki kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Na katika baadhi ya wakati wa Utawala wake Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* basi alikua akisoma Qunut kabla ya kurukuu kwa kusema kua: 'Wacha waliochelewa Sala ya Jamaa wawahi kabla Kurukuu. Hivyo huu ni Uthibitisho wa wazi kwa upande wa Madhhab yetu, mbali ya kua Wapinzani wetu wanatushambulia kwa Hadith isemayo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut kwa mwezi kisha akasita.'

Ambapo Hadithi hii inamaanisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisitisha Kuwaombea Dua ya Maangamizi Makafiri husika kama ilivyonukuliwa na Abd Rahman Ibn Mahdi.Ambae nae Msimamo wake juu ya hadith hii uko wazi, kwani alisema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisitisha Kuwalaani tu.'*(Sharh Al Wasit - Imam Ibn Salah Al Shafii)***

Kwani anasema Mujaddid Ad Din Mujtahid Imam Al Mudhhab Al Shafii Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Kuna Miongoni mwa watu wenye Ilm wameniambia mimi kua,kutoka kwa Jafar Ibn Muhammad kutoka kwa Baba yake ambae amesema kua:Wakati habari za Mauaji ya Watu wa Bir Maunah zilipomfikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* basi alikaa kwa Usiku wa siku 15 ambazo ndani yake ilikua kila akinyanyua Kichwa chake kutoka kwenye Rakaa yake ya Mwisho ya Salat Al Fajr alikua akisema:*Sami Allahu Liman Hamida, Rabbana walaka Al Hamd,* na kisha huanza kusoma Dua ndefu sana, kisha husema Allahu Akbar na kisha Husujudu.'**

Imam Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Amesema Jafar *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut katika Sala zote katika wakati ambao watu wa Bir Maunah walipouliwa.'**

'Na imenukuliwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut katika Salat al Maghribi. Na pia imenukuliwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut katika Sala Nyenginezo mbali ya katika Salat Al Fajir wakati watu wa Bir Maunahwalipouliwa...*Wa Allahu Aalam.'*

'Na pia amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwacha kusoma Qunut. Na kila alienukuu Hadith kama hii ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* basi anasema kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut wakati watu wa Bir Ma'unah walipouliwa na baada ya hapo akawacha kusoma Qunut.'

'Ama kuhusiana na Qunut ya Salat Al Fajr basi ilikua ikisomwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na katika wakati watu wa Bir Ma'unah walipouliwa na baada ya hapo, na haikusemwa kutoka kwa yeyote yule kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliachana nayo Qunut ya Salat Al Fajr.'

Kisha Imam Muhammad Idris Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Az Zuhri kua amesema Said Ibn Musayyib kua:**

أبي هريرة لما رفع النبي صلى الله عليه وسلم رأسه من الركعة الأخيرة من صلاة الصبح قال : اللهم أنج الوليد بن الوليد وسلمة بن هشام وعياش بن أبي ربيعة والمستضعفين بمكة اللهم اشدد وطأتك على مضر واجعلها عليهم سنين كسني يوسف.،

AmesemaAbu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akinyanyua Kichwa chake kutoka kwenye Rukuu ya Salat Al Fajr basi alikua akisema:

Allahuma Muokoe Al Walid Ibn Al Walid, Salamah Ibn Hisham, Ayyash Ibn Abi Rabiah na kila anaedhulumiwa katika Ardhi ya Makkah. Ya Allah Ifanye Adhabu yako iwe kali kwa Mudhar na wafanyie Miaka yao kua kama ilivyokua miaka ya Yusuf.'

Imam Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Ama kuhusiana na maneno ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliachana na Qunut basi Sijui alikua akimaanisha nini.'**

'Kwani mimi ninavyoona kulingana na Vitibitisho basi ni kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwacha kusoma Qunut katika Sala nne, isipokuaSala ya Alfajir, kama alivyosema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua

فُرِضَتِ الصلاةُ ركعتينِ ركعتينِ في الحضَرِ والسَّفَرِ فأُقِرَّتْ صلاةُ السَّفرِ وزيدَ في صلاةِ الحضَرِ

Sala iliFardhi shwa ikiwa katika Hali ya Sala ya Rakaa 2 Mbili katika Sala za Nyumbani na za Safari, na ilipothibitishwa Sala ya Safari basi Sala za Nyumbani zikaongezewa.'*(Sunan Al Qubra)*

Yaani Sala 3, Dhuhr, Asr na Isha ziliongezewa Rakaa 2, 2 isipokua Sala ya Maghrib iliongezewa 1 na Al Fajr ambayo iliachwa kama ilivyo.

Na kabla ya kuendelea basi tunaona hapa kuna Hadith ya *Aisha Radhi Allahu Anha* kuhusiana na Namna ilivyokua Ikisaliwa Sala hapo awali kua ilikua ni Rakaa mbili mbili kwa kila Sala, iwe Sala ya Safari pale Mtu anapokua Safarini njiani au Sala ya Nyumbani yaani Mtu anapokua Nyumbani katika Mji anaoishi.

Yaani Sala zote zilikua zikisaliwa Rakaa mbili mbili.Na hivyo baada ya Safari ya Miraj na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kufardhishiwa Ibafa ya Sala.Basi Sala za Nyumbani katika Mji anaoishi Mtu husika zikaongezewa Rakaa mbili mbili yaani pale anapokua hayupo Safarini kwa Salat Adh Dhuhr, Salat Al Asr na Salat Al Ishaa zikawa na Rakaa 4 baada ya kuongezewa Rakaa mbili. Ambapo Sala ya Al Fajir ikabakia kama ilivyokua na haikuongezewa Rakaa kwa sababu ya Urefu wa Kisomo chake ndani yake.

Na Sala ya Magharibi ikawa Rakaa 3 kwa sababu ndio Sala ya Witr ya Siku. Na hivyo Sala mbili hizi za Al Fajr na Maghrib hua hazifupishiki Rakaa hata katika wakati ambao Mtu anakua Safarini na kuruhusika Kufupisha Sala.

Ambapo inasemekana pia kua wakati Ras*ul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua amehamia Madina na kuishi ndani yake Mji huo alikua anaposafiri alikua akifupisha Sala zake.Na Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala Akashusha* Aya isemayo:

﴿فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ﴾

Falaysa Aaalaykum Junaahu An Taqsiruu Mina Al Salati *(Surat An Nisaa 4:101)*

*Tafsir :**Na Hakuna Kosa Juu yenu Kama Mkifupisha Sala.***

Ambapo Wanazuoni wanasema kua hii ni Aya yenye kuithibitisha Kufupisha Sala ya Safari kulingana na kuhitajika kwake Kufupishwa kutokana na Hali ya mazingira tofauti ya Msafiri anapokua Safarini.

Imam Al Shafii anaendelea kusema kua:**'Hivyo ndivyo ilivyokua na ilivyoachwa (katika Rakaa za Sala), hivyo kuhusiana na Qunut katika Salat Al Fajr basi haikutufikia sisi kua *Rasul Allah***

***Salallahu Alayhi wa Salam* aliachana nayo**.*'(Imam Al Shafii katika Kitabu chake cha Ikhtilaf Al Hadith)*

Kwani anasema Imam Anu Jafar Al Razi kua: '**Amesema Al Rabi Ibn Anas kua: Mimi nilikua nimekaa na Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na akaambiwa kua:Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alisoma Qunut kwa mda wa Mwezi mmoja Tu.**

Ambapo Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliendelea Kusoma Qunut katika Salat Al Fajr hadi kufariki kwake.'(*Sunan Al Kubra - Imam Al Bayhaqi)*

Imam Al Bayhaqi anaendelea kusema kuhusiana na Qunut ya Salat Al Fajr kua: **'Hadith hii pia imenukuliwa na Ubayd Allah Ibn Musa ambae amesema kua amesema Abu Jafar Al Razi kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* alisoma Qunut kwa mda wa Mwezi mzima akiwaombea Maadui, lakini kuhusiana na Salat Al Fajr basi alikua akisoma Qunut hadi alipoondoka Dunian**i.'*(Sunan Al Kubra)*

Naam..Imam Al Bayhaqi anatuambia kuhusiana na Hadith hii kua**: 'Hadith hii inaunga mkono Uthibitisho wa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na Vithibitisho vyenginevyo kwenye Vitabu vya Hadith.'**

Ambapo tunapomzungumzia Imam Al Rabi Ibn Anas basi alikua ni Tabiina Mwanazuoni aliekua akiishi katika Mji wa Basra, ambae alisoma kwa Makik Ibn Anas Radhi Allahu Anhu na pia akasoma kwa Imam Abu Aaliyah.Na miongoni mwa Wanafunzi wa Imam Al Rabbi basi niImam mwenye Taqwa na Uadilifu mkubwa,na Ilm kubwa sana ambae si mwengine bali ni Imam Abd Allah Ibn Mubarak.

Kwani anasema Imam Al Shafii katika Al Qadiim kua: **'Kuna Mtu ametuambia sisi kua amesema Ali Ibn Yahya kua amesema Hasan Al Basr kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Abu Bakr na Umar Radhi Allahu anhum walikua wakisoma Qunut katika Salat Al Fajr baada ya Rukuu ya Pili, na alipokuja Uthman ndio akaiweka Kabla ya Rukuu.'** Ambapo Imam Al Bayhaqi ameinukuu pia kauli hii ya Imam Al Shafii katika Sunan Al Kubra.

Na moja kati ya Vitabu alivyoandika Imam Al Shafii katika kuikosoa Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa, basi ni kile kitabu kiitwacho Ikhtilaf Al Iraqiyyin ambacho Imam Al Shafii amesema ndani yake kua: **Abu Hanifa amekataza Qunut katika Salat Al Fajr, na Abu Yusuf akafuata Mfano wake, kwa kunukuu Hadith kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakusoma Qunut**. **Isipokua kwa mda wa Mwezi mmoja, alipopigana na Washirikina na kisha akawasomea Qunut kuwalaani.**

Na kwamba Abu Bakr Radhi Allahu Anhu **hakusoma Qunut hadi alipokutana na Mola wake**. **Na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* hakusoma Qunut alipokua Nyumbani wala alipokua Safarini.**

Na kwamba Umar, wala Ibn Abbas wala Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum*Na akasema; Enyi watu wa Iraq nimesikia mimi kua Imam wenu nyinyi hasomi Qunut. **Na kua Ali Ibn Abi *Talib Radhi Allahu Anhu* alisoma Qunut katika wakati wa Vita akimlaani Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu,*na hivyo watu wa Mji wa Kufah nao wakamuiga.**

Na Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* alikua akisoma Qunut katika Ardhi ya Sham akimlaani Ali Ibn Abd Mutallib *Radhi Allahu Anhu,* na Hivyo watu wa Sham nao wakamuiga.

Ambapo anasema Abd Rahman Ibn Abi Layla alikua akisoma Qunut katika Salat Al Fajr baada ya Kisomo cha Qur'an kabla ya Kurukuu na alikua akisema kua Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alikua akisoma Qunut kwa kusema:

" اللهم إنا نستعينك، ونستغفرك، ونثني عليك الخير، ولا نكفرك، ونخلع ونترك من يفجرك، اللهم إياك نعبد ولك نصلي، ونسجد، وإليك نسعى ونحفد، نرجو رحمتك، ونخشى عذابك، إن عذابك بالكفار ملحق

*Tafsir: **Ya Allah, Tunakuomba msaada wako na tunaomba msamaha wako, na Tunakutukuza kwa mema yako, na sisi si wenye kutokuamini wewe na tumeachana na wanaokukufuru, Ya Allah ni wewe tu ndie mwenye kustahiki kuabudhiwa, nasi tunasali kwa kukuelekea wewe na tunasujudu kwa kukuelekea wewe, na tunajitahid na tunakimbilia huku tukitumainia Rehma zako kwani tunaogopa Adhabu zako kwani adhabu zako zitawafika wenye kukufuru.***

Hivyo kuhusiana na Salat Al Fajr, basi mimi simjui Mtu ambae aliachana na Qunut ndani yake, hivyo kila anaesali anatakiwa aisome.

Na anasema Imam Al Bayhaqi kua:**'Amesema Abu Said Ahmad Muhammad Al Harawi kua AbdAllah Ibn Afi Al Hafidh kua amesema Zakarriyah Ibn Yahya Al Saji ku amesema Bandar kua amesema Yahya Ibn Said kua amesema Al Awwam Ibn Hamza kua:Mimi nilimuuliza Abu Uthman kuhusiana na Qunut katika Salat Al Fajr.'**

Ambapo nae akasema kua: 'Ni baada ya Kurukuu'

Nami nikamuuliza: 'Kutoka kwa Nani hayo?'

Ambapo Nae akasema: 'Kutoka kwa Abu Bakr, Umar, na Uthman *Radhi Allahu Anhum'(Sunan Al Kubra)*

Imam Al Bayhaqi amaendelea kusema kua**: 'Ametuambia sisi Abu Abd Allah kua amesema Abu Al Abbas kua Al Hasan Ibn Ali Ibn Affan amesema kua, ametuambia Muhammad Ibn Bishr kua amesema Said kua amesema Qatadah kua amesema Al Hasan kua amesema Abu Rafii kua:Umar akikua akisoma Qunut katika Salat Al Fajr.'**

Imam Al Bayhaqi anaendelea kusema kua: **'Hivi ni vithibitisho vilivyo sahih juu ya kusomwa kwa Qunut Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* kama tulivyoainisha katika vithibitisho vya Sunnah Hapo Kabla.'**

Kwani amesema pia Imam Al Shafii kua: '**Tumeambiwa sisi kua amesema Jafar Ibn Muhammad kua amesema Baba yake kua:** '**Ali Ibn Abi Talib Radhi Allahu Anhu alikua akisoma Qunut katika Rakaa ya mwisho ya Salat Al Fajr.'**

Na pia tumeambiwa kua amesema Yazid Ibn Ziyad kua amesema Abd Rahman Ibn Layla kua: '**Ali Ibn Abi Talib Radhi Allahu Anhu alikua akisoma Qunut katika Salat Al Fajr baada ya Kurukuu.'**

Na pia amesema Abu Said kua amesema Abu Al Abbas kua**'Amesema Al Rabbi kua amesema Al Shafii kua:Nimemsikia mimi Hisham akisema kua amesema Husayh kua amesema Ibn Mughafili kua:** '**Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alikua akisoma Qunut katika Salat Al Fajr.'**

Ambapo Imam Sufyan Ath Thawry amenukuu hadith hii kupitia kwa Abu HusaynKutokea kwa Abd Allah Ibn Maqil kua Ali Ibn Abu Talib *Radhi Allahu Anhu* alikua akisoma Qunut katika Salat Al Fajr.

Hivyo Imam Al Bayhaqi anaendelea kusema kua:**'Hakuna haja ya kukataa hoja za Wale wanaokataa Qunut katika Salat Al Fajr na hii ni kwa sababu Hukmu yake Jambo hili hua ni Kulingana na Walioshuhudia na Waliosikia na wala si kulingana na Kauli za wale ambao hawakushuhudia wala hawakuona.Kwani Sanad ya Hadith isemayo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisoma Qunut kwa Mwezi mmoja na kisha hakusoma tena dhidi ya yeyote, ni Hadith yenye Sanad isiyokua na Nguvu wakati sisi Tumenukuu Hadith zenye Vithibitisho Sahih na vyenye nguzu zaidi.'**

Tumalizie Mada hii kwa kukumbushana kua Miongoni mwa Maimam wa Tabiina waliokua na Ilm Kubwa ya Fiqh Hadith, Quran, Ndoto na Hadith zenye Duaa basi hakuna kama Imam Muhammad Ibn Sirin. Ambae yeye ndie aliemuuliza Sahaba Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kama asemavyo Imam Al Bayhaqi katika Hadith ifuatayo: '**Qadhi Abu Is-haq ametuambia sisi kua amesema Imam Al Shafii kua amesema Abu Jafar; kua amesema Imam Muhammad Ibn Sirin kua:Mimi nilimuuliza Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Qunut ambapo nae akasema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhu wa Salam* alisoma Qunut baada ya Rukuu.'**

Ambapo Hadith hii pia ameinukuu Imam Al Muzani kutoka kwa Imam Al Shafii kupitia kwa Abd Al Wahhab Ibn Abd Al Majid kupitia kwa Imam Ayub Al Sakhtiyani kutoka kwa Imam Muhammad Ibn Sirin.

Na pia Imam Abu Ali Al Rawz Al Bari amesema kua amesema Abu Bakr Ibn Dasa kua amesrma Abu Daud kua amesema Imam Sulayman Ibn Harb kua amesema Imam Hammad Ibn Yazid kua amesema Imam Ayub Al Sakhtiyani kua amesema Imam Muhammad Ibn Sirin.

Kwani ni Jambo lisilokua na Shaka kuhusiana na Kuthibitishika na Kukubalika kwa Sunnah Abaadh ya Kisomo cha Qunut kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii.Ambapo Imam Muhammad Idria Al Shafii Mwenyewe amethibitisha juu ya hilo takriban katika kila kitabu chake cha Hadith na Fiqh akichoandika. Kuanzia kwenye Al Risala, kwenye Ikhtilaf Al Iraqiyiin, kwenye Ikhtilaf Al Hadith, kwenye Ikhtilaf Shafii wa Maliki, kwenye Ukhtilaf Ali wa Ibn Masud *Radhi Allahu Anhum, kwenye* Al Umm, kwenye Maarifat Sunnat wa Al Athar n.k.

Na hivyo Imam Al Shafii kua ni mwenye kutuwekea wazi kua: '**Wale wanaosema kua Qunut ilisomwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha ikasitishwa kua hawakufaham**. **Kwani Qunut iliyositishwa ni ya Maombi ya Katika Sala nyenginezo za Fardhi isipokua Sala ya Al Fajr, katika wakati wa Mitihani na wala si Qunut ya Salat Al Fajr.**

Ambapo Mtizamo huo pia umepitiwa na Wanazuoni wa Fkqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuoingana na vithibitisho vyake na kisha kuthibitishwa na Maimam wote wakubwa wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii, na hivyo kua ndio Qawl Al Mutammad yaani Qauli inayokubalika katika Madhhab ya Imam Al Shafii.'

Na hivyo kuna Makubaliano ya wazi kua akataeisahau, au atakeiwacha kwa makusudi Qunut ya Salat Al Fajr basi hua na Wajibu wa Kuleta Sijdat Al Sahw mwishoni mwa Sala yake.

Kwani anasema Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Farra Al Baghawi Al Shafii kua: '**Kauli inayokubalika zaidi katika Madhhab yetu miongoni mwa As-hab wetu basi ni**

kua:Qunut inatakiwa kusomwa baada ya Dhikr ya kawaida ya Sala ya kutoka kwenye Rukuu yaani *Sami Allahu Liman Hamida, Rabban walaka Al Hamd* na hivyo baada ya hapo unaweza kuomba Ukitakacho.'

Ambapo Mtizamo huo ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii, Imam Al Muzani, Imam Al Isfarini, Imam Al Ghazali, Imam Al Rafi, Imam An Nawawi, Imam Al Isnawi, Imam Al Ramli wote wawili, Imam Ibn Hajar wote wawili, Imam Zakrriyah Al Ansari, Imam Al Qastallani, Imam Al Subki wote wawili, Imam Al Shirbini, n.k.

Ambapo kwa upande wa Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Qunut hua ni yenye kusomwa baada ya mtu kumaliza kusema *Sami Allahu Liman Hamida, Rabbana wa laka Al Hamd,* kisha ndio inafuatia Qunut.'**

'Ila kama Mtu atakua amemfuata Imam ambae anasoma Qunut kabla ya Rukuu basi nae atasoma kabla ya Rukuu na kisha haitomhitajia mtu huyo kusoma tena Qunut baada ya Rukuu kwa sababu kulingana na utofauti wa Mtizamo wa Wanazuoni basi Qunuti hio hua imemtosheleza'

Na anasema Imam Taj Ad Din Al Fazari Al Farkah Al Shafii katika Kitabu chake cha Al Iqlid kua: '**Usomaji Qunut na *Dhikr Allah* za kutoka kwenye Rukuu hua ni kulingana na makisio, kwani hapa kama itamaanisha kua Qunut inaunganishwa na Dhikr Allah, na hivyo sehemu ya Dhikr Allah itakua ni ndefu, wakati Dhikr Allah ya hapa hua inahesabika kua ni Miongoni mwa dhikr fupi za Sala na hili ni jambo ambalo halina kutofautiana juu yake.Hivyo basi hua haipendezi kuunganisha Dhikr Allah hizi na Qunut.'**

Ama kwa upande wa Imam Kamal Ad Din Muhammad Ibn Musa Al Damiri Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Hakuna Tatizo kuunganisha Dhikr Allah na Qunut, na hua ni Sahih kama alivyosema Al Baghawi.'**Na huo pia ndio Mtizamo wa Imam Shams Ad Din Al Ramli katika Al Nihayat na Imam Al Shirbini katika Al Mughni.

Na hapa inabidi tujue ili tusichanganye majina kwani kuna Imam Ad Damiri Al Shafii ambae ni Mzaliwa wa Misri mwaka 742 A.H, na pia kuna Imam Ad Darimi Al Shafii ambae ni mzaliwa wa Samarqand - Uzbekistan mwaka 181 A.H. Ingawa wote ni Wanazuoni wakubwa sana na wanaotisha kielimu lakini tunaemzumzia hapa ni Ad Damiri ambae ni Mwanafunzi wa Imam Al Isnawi, Imam Ibn Aqil, Imam Al Subki, Imam Al Bulqini, Imam Al Iraqi n.k.

Kabla ya kuingia katika mada ya Mufarraqat basi tuangalie miongoni mwa Masuali ambayo Watu wanayoweza kujiuliza kuhusiana na Qunut ya Salat Al Fajr. Ambalo ni kua: **'Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik basi Kama Maamuma mwenye hali ya kua ni Masbuq yaani aliechelewa kufika Msikitini katika Jamaa ya Salat Al Fajr na akamkuta Imam akiwa katika Rakaa ya pili ambapo kwake yeye Maamuma huyo Rakaa hio itakua ni ya kwanza, na ikasomwa Qunut na Imam husika na Maamuma huyo akaitikia Qunut hio, basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanasema kua Qunut hio humtosheleza Maamuma huyo.**

Hivyo Jee kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hukmu yake inakuaje? Jee Maamuma huyo atatakiwa kusoma Qunut katika Rakaa yake ya pili ama Qunut iliyosomwa na Imam katika Rakaa ya kwanza ya Maamuma aliechelewa itamtosheleza kama wasemavyo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik?'

Naam, kwanza tunapoangalia vithibitisho vya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik katika Hukmu yao hii basi tunaona kua wametumia Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:**Amesema R*asul Allah Salallah Alayhi wa Salam* kua:**

"إذا سمعتم الإقامة فامشوا وعليكم السكينة والوقار، ولا تسرعوا، فما أدركتم فصلوا، وما فاتكم فاقضوا

'Itakapokimiwa Sala, basi Msiende kwa kuikimbilia, bali nendeni kwa mwendo wa kawaida na utulivu'Mtakachokipata Katika Sala basi Salini, na mtakachokikosa basi *Fa-aqadhaw* (Lipeni.)'*(Abu Daud, Al Nasa'I,Imam Ahmad, na imethibitishwa na Ibn Hibban)*

Ambapo hadithi hii ndani yake imetumia neno *Fa-aqadhaw(Hivyo na alipe)* ambalo hua ni lenye kuamrisha kuashiria amrisho linalomtaka mtu husika kulipa kile kilichokosekana katika Sala yake

Hivyo kulingana na hadith hii basi tunaona kua katika hali kama hii hua inaruhusika kwa Maamuma Masbuq ambae ameiwahi Qunut katika Rakaa ya pili ya Sala ya Jamaa na kisomo hicho cha Qunut hio cha Imam hua kinamtosheleza,na haina haja kwake Maamuma kuirudia au kuilipa Qunut, kwani hakuikosa ndani ya Sala yake.

Na huo ndio mtizamo wa Imam Abu Hanifa, Imam Malik, Imam Sufyan Al Thawri na Ahmad Ibn Hanbal ambao wao wamesema kua: **'Kile alichokiwahi Maamuma Masbuq hua ni sahemu ya mwanzoni mwa Sala yake, na kile anachokilipa hua ni sehemu ya mwishoni mwa Sala yake'**

Na imenukuliwa hivyo pia kutoka kwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Imam Ibn Al Mundhiri, Imam Mujahid na Imam Muhammad Ibn Sirin.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi anasema Imam Shams Ad Din Al Ramli kuhusiana na Hadith hii kua: '**Neno Qadhaa ilitumika kwenye hadithi hii limetumika katika kumaanisha mtizamo wa Kilugha tu, na hii ni kwa sababu a kutokana na matumizi ya majaz kimaana kua ni yenye kutumika sana, ambapo maana halisi ya neno Qadha iliyotumika hapa basi ni amrisho la kusema: 'Irudieni Rakaa' na wala si kusema 'Ibadilisheni Rakaa husika iliyokosekana kwa Rakaa nyengine'**

Na pia kwa upande mwengine basi tunaona kua haiwezekani kwa neno Qadha lilivyotumika hapa kua sawa na maana ya neno Shara kimtizamo kwa sababu hakuna maingiliano ya moja kwa moja kimaana na hali ya tukio huska linalozungumziwa kwenye hadith hii, kwani Sala inayozungumziwa hapa ni ile ambayo bado imo ndani ya wakati wake na wala si nje ya wakati wake.'(*Nihayah Al Muhtaj fi Sharh Al Minhaj*)

Imam Al Ramli anaendelea kusema kua Hivyo Mtu aliewahi Qunut ya Rakaa ya pili ya Sala ya Jamaa ya Salat Al Fajr ambayo kwake yeye hua ni Rakaa ya kwanza hua anatakiwa kuirudia Qunut katika sehemu yake husika ambayo ni kwenye Itidal ya Rakaa ya pili, kwa sababu Qunut ya kwanza aliisoma kwa ajili ya kumfuata Imam wakati yeye mwenyewe katika Sala yake ilikua haujaingia bado wakati wa kusoma Qunut na hivyo Maamuma asingeweza kuisoma Qunut katika Rakaa yake ya kwanza kama angekua anasali peke yake.'(*Nihayah Al Muhtaj fi Sharh Al Minhaj*)

Kwani Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii anasema kua: **'Kilichoelezwa na hadithi hii ni kutokana na msingi wa kua pale inapokua Maamuma Masbuq ni mwenye kumuwahi Imam, lakini katika mwanzoni mwa Sala yake yeye Maamuma na hivyo kile anachotakiwa kukimalizia ni mwishoni mwa Sala yake yeye Maamuma'**

Ambapo Shaykh ul Islami Imam AbuZakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi anasema kua: **'As-hab zetu wamenukuu uthibitisho wa Hadith isemayo: 'Chochote kile atakachokiwahi Mtu katika Sala basi amekiwahi na alichokikosa basi na akikamilishe.' Kama Ilivyonukuliwa na Imam Bukhari n a Muslim kwa Sanad nyingi zaidi**''

'Hivyo tumesema hapo kabla kua kulingana na Mtizamo wetu ni kua Maamuma Masbuq (aliechelewa) anapoiwahi sehemu ya awali ya Sala basi hua nimwenye kutakiwa kuimalizia ni sehem ya mwisho ya Sala yake na huo ndio mtizamo wa Imam Sayyid Ibn Mussayyib, Hasn Al Basr, Ataa, Umar Ibn Abd Al Aziz, Makhul, Al Zuhri, Al Awzai, Said Ibn Aba Al Aziz na Is-haq. Ibn Al Mundhiri amenukuu kutoka kwao na kusema kua Huu ndio Mtizamo wangu na kisha akasema: 'Hivi ndivyo pia ilivyonukuliwa na Umar, Ali na Abu Darda *Radhi Allahu Anhum* lakini haikuthibitishwa na pia imenukuliwa kutoka kwa Malik na ndio Mtizamo wa Daud''

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawianaendelea kusema kua: **'Katika hali hii Rakaa inayounganishwa na Masbuq Maamuma kwake yeye hua ni Rakaa ya Kwanza, hivyo Maamuma huyu hua anatakiwa airudie Qunut katika Rakaa yake ya pili'***(Minhaj Al Talibin wa 'Umdah Al Muftin)*

Na kwa upande wa Imam Ibn Al Naqib basi yeye amesema kua: **'Baada ya rakaa ya mwisho ya Salat Al Fajr ya Imam ambayo kwa Maamuma Masbuq hua ni rakaa ya kwanza, basi Maamuma atanyanyuka na kumalizia Rakaa yake ya pili, na hivyo Maamuma huyo husika atatakiwa kurudia kisomo cha Qunut katika Sala yake hio** *' ('Umdah Al Salik wa 'Uddah Al Nasik)*

Na kwa upande wa Shaykh Islami Imam Zakariyyah Al Ansari amesema kua: '**Katika hali kama hii basi Rakaa ya mwisho ya Imam hua ni yenye kuendasambamba na Rakaa ya kwanza ya Maamuma, hivyo wakati Maamuma anaponyanyuka ili kumalizia Sala yake basi hua anatakiwa kurudia kisomo cha Qunut kama Sala hio ikiwa ni Sala ya Al Fajir, na kama ikiwa ni Sala ya Magharibi basi Maamuma itambidi kurudia Tahiyyat ya mwisho ya Sala hio ya Magharibi'**(*Fath Al Wahhab bi Sharh Minhaj Al Tullab*)

Kwa sababu amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

إذا أُقيمتِ الصلاةُ فلا تأتُوها و أنتم تسعون ، و أتوها و أنتم تمشون ، و عليكم السكينةُ ، فما أدركتُم فصلُّوا ، و ما فاتكم فأَتِمُّوا

'Itakapokimiwa Sala, basi Msiende kwa kuikimbilia, bali nendeni kwa mwendo wa kawaida na utulivu na Chochote kilemtakachokiwahi katika Sala basi mmekiwahi na mlichokikosa basi *Faatimuu* (mkikamilishe).'*(Sahih Bukhari na Sahih Muslim)*

Ambapo hadithi hii ndani yake imetumia neno *Fa-atimu (Hivyo na akamilishe)* ambalo hua ni lenye kuamrisha kuashiria amrisho linalomtaka mtu husika kukamilisha Sala yake katika utaratibu unaotakiwa.

Na Shaykh Islami Imam Zakariyyah Al Ansari anaendelea kusema kua: **'Imam Al Bayhaqi basi anasema kuhusiana na Hadith hii kua: 'Wale walionukuu Hadith yenye neno Akikamilishe wako wengi zaidi na ni wenye kua na sifa ya kua na Ufaham mzuri zaidi na wako karibu na Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*ambae ndie alieinukuu Hadith hii, hivyo wao ndio wako sahihi zaid'**

Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafiiamesema kua: 'Kumalizia kitu hua kunawezekana kufanyika pale inapokua tayari sehemu ya mwanzo ya kitu imeshafanyika' na Imam Al Bayhaqi amenukuu pia Mtizamo kama wetu kutoka kwa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* kwa Abu Darda *Radhi Allahu Anhu,*Imam Ibn Musayyib, Imam Hasan Al Basr, Imam Ataa, Imam Ibn Sirin na Imam Abu Qilabah.'

Na ndivyo pia alivyosema Shaykh Abu Hamid kua: 'Kilichomaanishwa hapa ni kua Ulichokikosa hua ni katika Sala yako, na wala si katika Sala ya Imam wako, hivyo Maamuma Masbuq hua ni mwenye kuikosa sehemu ya mwisho ya Sala yake.'*(Al Majmuu)*

Hivyo wapokezi wa hadithi iliyotumia neno "Faati'mu" ni wengi na wajuzi zaidi kuliko wapokezi wa hadith iliyotumia neno *"Faqadha"*, na pili, kwamba qadha' inafasiriwa kuwa ni kitendo, sio qadhah. ' inayojulikana katika istilahi, kwa sababu hii ni istilahi ya mafaqihi wa baadae, na Waarabu wanatumia neno qadha' kumaanisha kitendo.

Ambapo kwa upande mwengine basi Neno Qadha ambalo katika hadithi hii limetumika kumaanisha Kukamilisha Kitendo basi limetumika pia katika Qur'an kumaanisha Kukamilisha Kitendo pale ziliposema aya:

﴿فَإِذَا قَضَيْتُمْ مَّنَاسِكَكُمْ فَٱذْكُرُواْ ٱللَّهَ كَذِكْرِكُمْ آبَآءَكُمْ أَوْ أَشَدَّ ذِكْراً فَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَقُولُ رَبَّنَآ آتِنَا فِي ٱلدُّنْيَا وَمَا لَهُ فِي ٱلآخِرَةِ مِنْ خَلاَقٍ﴾

Fa-idha qadaytum manasikakum faodhkuroo Allaha kadhikrikum abaakum aw ashadda dhikran famina alnnasi man yaqoolu rabbanaatina fee alddunya wama lahu fee Al akhirati min khalaqin*(Surat AlBaqarah 2:200)*

Tafsir: ***Hivyo mtakapomaliza Manasik yenu (Ihram, Tawaf, Sai baina ya Safa na Marwa, Kikao cha Arafa, Muzdaliffat na Mina, kurembea Mawe katika Jamarat na Mina) basi chinjeni Mnyama na Mumkumbuke Allah Subhanah wa Ta'ala kama walivyokuwa wakikumbuka Mababa zenu waliotangulia au kwa wingi zaidi. Ama kwa wale Watu wasemao : 'Ewe Mola etu tupe hapa Duniani' basi Hawatokua na chao Akhera.***

Na pale ziliposema aya

﴿فَإِذَا قَضَيْتُمُ ٱلصَّلاَةَ فَٱذْكُرُواْ ٱللَّهَ قِيَاماً وَقُعُوداً وَعَلَىٰ جُنُوبِكُمْ فَإِذَا ٱطْمَأْنَنتُمْ فَأَقِيمُواْ ٱلصَّلاَةَ إِنَّ ٱلصَّلاَةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَاباً مَّوْقُوتاً﴾

Fa-idha qadaytumu alssalata faodhkuroo Allaha qiyaman waquAAoodan waAAala junoobikum fa-idha itma/nantum faaqeemoo alssalata inna alssalata kanat AAala almu/mineena kitaban mawqootan*(Surat AlNisa 4:103)*

Tafsir: **Matakapomaliza Sala, basi Mkumbukeni Allah mkiwa Mmesimama, Mmekaa, Mmelala kiubavu, lakini Mnaopkua huru kutokana na Hatari, basi Simamisheni Sala kwani kwa hakika Sala Imeamrishwa kwa Waumini katika Wakati Maalum.**

Na pale ziliposema aya

﴿فَإِذَا قُضِيَتِ ٱلصَّلَاةُ فَٱنتَشِرُواْ فِي ٱلأَرْضِ وَٱبْتَغُواْ مِن فَضْلِ ٱللَّهِ وَٱذْكُرُواْ ٱللَّهَ كَثِيراً لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Fa-idha qudhiyati alssalatu faintashiroo fee Al ardhi waibtaghoo min fadhli Allahi waodhkuroo Allaha katheeran laAAallakum tuflihoona*(Surat Al Jumuah 62:10)*

Tafsir: **Hivyo Itakapomalizika Sala (ya Ijumaa) basi mnaweza kutawanyika Ardhini kwa ajili ya kutafuta Riziki za Allah na Kumkumbuka Allah kwa wingi ili mpate kua wenye Kufuzu.**

MUFARRAQAH NA HUKMU YAKE KATIKA SALA

❖❖❖

Hivyo katika kuangalia kuhusiana na Qunut katika Salat Al Fajr na tunaona kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii baada ya kuthibitisha kua ni Sunnan Ab'aadh ya Sala yaani Sunnah ya Wajib ambayo kutoitekeleza kwake hukubidi kuleta Sijdat Sahw kutokana na kua na Kasoro ndani yake. Na katika Kuzungumzia kwao basi Wanazuoni wanasema kua ni vizuri kutoijumuisha au kutoifungamanisha pamoja Dua ya Qunut na Dhikr za Itidal yaani Kisimamo cha baada ya Rukuu.

Na ingawa inafaa kufanya hivyo na hakuna tatizo lolote kama alivyosema Imam Al Baghawi lakini ni bora kutofautisha kwa kusita kidogo baada ya Dhikr kabla ya kuanza kisomo cha Dua ya Qunut.

Na pia amesema Imam Dhiau Al Din Abd Al Malik Ibn Yusuf Al Juwayni Al Haramayn Al Shafii kua: **'Itidal ni Nguzo Fupi ya Sala na inatakiwa kufupishwa na hivyo kama Mtu akiirefusha kwa mfano kwa kukaa kimya, kwa kusoma Qunut (ndefu) isiyokua ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* au kwa Dhikr Nyengine basi hua kunabatilisha Sala.'**

Ambapo mbali ya kua huo ndio pia Mtizamo wa Imam Abu Muhammad Ibn Husayn Ibn Masud Al Baghawi Al Shafii kama ilivyoelezewa na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyah Ibn Sharaf An Nawawi katika *Al Majmuu.*

Lakini pia kuna mtizamo mwengine ambao ndio unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ndio Mtizamo wa *Qawl Al Mutammad* unaotokana na msingi wa kua Dhikr za *Al Itidal Al Qawma* hua ni yenye Dhikr fupi ndani yake na hivyo kuhusiana na Urefu wa Kisomo cha Qunut basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Hua ni Makruh Kuirefusha Qunut, katika Sala ya Al Fajiri kama vile ilivyokua ni Makruh Kuirefusha Tahiyyat ya Kwanza ya Sala'***(Al Majmuu)*

Ambapo mtizamo huu wa Imam An Nawawi ni wenye kutokana na Mtizamo wa Imam Al Baghawi ambae yeye hakusema kua inakitihisha bali amesema kua **'Inachukiza kuirefusha Qunut ya Sat Al Fajr kama vile inavyochukiza Kuirefusha Tahiyyat ya mwanzo ya Sala.'**

Na tunapomuangalia Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari katika *Asna Matalib* basi tunaona kua nae amesimamia kwenye Mtizamo wa Imam An Nawawi kwa kusema kua: '**Katika Skuli ya Madhhab yetu ya Al Shafii, basi hukmu ya kuirefusha Qunut ya Sala ya Alfajir zaidi ya kustahiki kwake, ambako ni kama alivyosoma *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,*hua ni Makruh.'**

Na mtizamo huo ndio mtizamo wa Imam Al Ramli pia ambae amesema kua: '**Hua ni Makruh kuirefusha Qunut kama vile ilivyokua ni Makruh kuirefusha Tahiyyat ya mwanzo, na hua ni Sunna kuijumuisha Qunut ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Qunut ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* kwa wale wenye kusali peke yao, au kwa Imam anaekubaliana na Maamuma wake watakaoridhika na kisomo kitakachotokana na urefu wa Qunut hio.'***(Ghayan Al Bayan)***

Na akasema Imam Sulayman Al Bajuri: '**Na inakirisha na haipendezi kuongezea katika Tahiyyat ya mwanzo na hii kwa sababu inatokana na msingi wa kua ni fupi ya kati na kati na haipendezi pia kuirefusha Qunut kama vile ambavyo haipendezi kuirefusha Tahiyyat ya Kwanza ya Sala'***(Hashiyat Al Baijuri)*

Nakutokana na kukubaliana kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Ni Makruh kuirefusha Qunut ya Sala ya Al Fajir, basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanakubaliana pia kua: '**Inakubalika kwa Maamuma Kua Mufarraqah pale inapokua Imam anasoma Qunut ndefu katika Sala ya Al Fajr.'**

Na kabla ya kuendelea mbele zaidi basi na tufahamishane kuhusiana na asili na maana ya Mufarraqah. **Ambapo Neno Mufarraqah linatokana na neno Faraqah ambalo humaanisha Kutenga, Kubagua, Kutokukubaliana, Kugawa,Kutofautisha.**

Neno Faraqah ndio lililotoa neno Mufaraqah ambalo Humaanisha Maamuma anaeamua Kujitenga kutokana na Kumfuata Imam wakati akiwa ndani ya Sala ya Jamaa inayoendelea kusaliwa kwa sababu zinazokubalika Kisharia.

Ambapo miongoni mwao ni kama tutakavyoona kua ni kuhusiana na Imam Kusoma Qunut ndefu ndani ya Salat Al Fajr.

Ama tunapoangalia kuhusiana na asili ya *Mufarraqah* na msingi wake basi ni kutokana na matukio kadhaa yaliyotokea katika wakati wa Rasul *Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ikiwemo Hadith ya Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* kama ilivyoelezewa katika Bukhari na Muslim ambayo inasema:

أَخْبَرَنَا قُتَيْبَةُ، قَالَ حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ، عَنْ جَابِرٍ، قَالَ صَلَّى مُعَاذُ بْنُ جَبَلٍ لأَصْحَابِهِ الْعِشَاءَ فَطَوَّلَ عَلَيْهِمْ فَانْصَرَفَ رَجُلٌ مِنَّا فَأُخْبِرَ مُعَاذٌ عَنْهُ فَقَالَ إِنَّهُ مُنَافِقٌ . فَلَمَّا بَلَغَ ذَلِكَ الرَّجُلَ دَخَلَ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَأَخْبَرَهُ بِمَا قَالَ مُعَاذٌ . فَقَالَ لَهُ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " أَتُرِيدُ أَنْ تَكُونَ فَتَّانًا يَا مُعَاذُ إِذَا أَمَمْتَ النَّاسَ فَاقْرَأْ بِالشَّمْسِ وَضُحَاهَا وَ { سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الأَعْلَى } وَ { وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَى } وَ { اقْرَأْ بِاسْمِ رَبِّكَ }

Na amesema Qutaybah kua amesema Al Layth kua amesema Abu Zubayr kua amesema Jabr Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua:Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* alisalisha Watu wake katika Sala ya Isha, na kisha ndani yake akasoma Sura Ndefu(Ambapo kuna Baadhi wanasema kua Alisoma Surat Al Baqara)

Hivyo mmoja kati ya Maamuma alipoona kua Muadh *Radhi Allahu Anhu* anasoma Sura ndefu, basi akakata Jamaa na kuamua Kusali peke yake. Kisha akamaliza kusali kabla ya Sala ya Jamaa na akatoka Msikitini na kuenda zake.

Na baada ya Sala watu wakamwambia Muadh kua kuna Mtu amekata Sala ya Jamaa na amesali peke yake. Muadh akasema kua: 'Mtu huyo ni Mnafiq.'

Hivyo habari hizo za kuambiwa kwa Mtu huyo ni Mnafiq zilipomfika mwenyewe alieitwa Mnafiq kwa kukata Sala na Kusali peke yake. Basi Mtu huyo akatoka na kuenda Kushtaki kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na aliyayasema Muadh juu yake baada ya Muadh Kusoma Sura ndefu na yeye akaamua Kukata Sala na kusali peke yake kwa Sababu ana shughuli nyengine ya kuwashughulikia Wanyama wake.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwita Muadh aje kujibu Mashtaka hayo. Na Muadh alipofika Mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kujieleza basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwangalia Muadh kisha akamwambia kwa kurudia Mara tatu kusema kua:Ewe Muadh! Jee unataka kuwafanyia Watu Mtihani katika dini yao?

Ewe Muadh! Unaposalisha Watu katika Sala basi Soma *Washamsi Wadhuhaha, Sabihisma Rabbika Al Aala, Walayli Ifha Yaghsha au Iqraa Biismi Rabbika*.'*(Bukhari na Muslim, Sunan An Nasai)*

Ambapo anasema Shyakh ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: **'As-hab wetu na wengineo wanaitumia hadith hii kua ni uthibitisho wa kua inakubalika kwa Maamuma kuachana na Sala anayosalishwa na kumalizia kusali Sala yake peke yake'***(Sharh Sahih Muslim)*

Hivyo kutokana na Hadith hii basi Wanazuoni wametoa Hukmu kua Mufarraqah hua ni Mubah yaani inakubalika lakini pale inapokua kuna sababu inayokubalika kisharia.

Naam..hivyo kulingana na tukio la Hadith ya Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu,* basi Wanazuoni wametoa Hukmu ya kua inaruhusika kwa Maamuma kua ni Mufarraqah kutokana na sababu zinazokubalika Kishariah.

Ambapo Sababu hizo zinazopelekea kukubalika kwa Mufarraqah basi ni:

1-Imam katika Kusalisha kwake amekua ni mwenye kusoma Sura ndefu au Qunut ndefu huku Maamuma wake wakiwa katika hali ya kua na wasiwasi juu ya Usalama wao au mali zao kutokana na kua na hali ya hatari ya Maangamizo.

2-Maamuma kua ni Mwenye kupatwa na Maradhi katika wakati ambao Ibada ya Sala ya Jamaa inaendelea.

3-Imam kufikwa na Tatizo ambalo litampelekea kuibatilisha Sala ya Jamaa, na Maamuma kua ni mwenye kujua kuhusiana na Dharura hio.

Kwani Wanazuoni pia wameigawa hali ya Mufarraqah kihukmu katika haki zifuatazo:

1-*Mufarraqah* hua ni *Wajib* pale Maamuma anapomuona Imam anafanya Jambo ambalo linabatisha Sala husika.

2-*Mufarraqah* hua ni *Sunna* pale Imam anapokua ni mwenye kuachana na Sunnah inayotiliwa Mkazo.

3-*Mufarraqah* hua ni *Mubah* yaani inaruhusika pale Imam anapokua anasoma Kisomo kirefu cha Qur'an au Dua kiasi ya kua Maamuma hawezi kuendelea kustahili zaid.

4-*Mufarraqah* hua *Makruh* yaani inakirihisha pale inapokua hakuna dharura au sababu inayokubalika kisharia kuachana na Sala ya Jamaa. Kwani hua ni Kujitoa ndani ya Sala ya Jamaa bila ya kua na sababu inayokubalika na hivyo kuivunjia haki yake Sala ya Jamaa.

5-*Mufarraqah* hua ni *Haram* pale inapokua kufanya hivyo kutapelekea kuvunjika kwa Umoja wa Kiislam katika Jamii na kusitisha maendeleo ya Dini ya Kiislam, au pale inapokua Jamaa hio ni ya Lazima kwa mfano Jamaa ya Sala ya Ijumaa.

Ambapo anasema Imam Shams Ad din Muhammad Ibn Muhammad Al Khatib Ash Shirbini Al Shafii kua: '**Miongoni mwa mambo yanayoweza kumpelekea Maamuma kua Mufarraqah ni Kisomo Kirefu ambacho kitampelekea Maamuma Kutoshindwa kustahmili kutokana na Dharurah ya Udhaifu wa Kiafya au Kua na Majukumu ya Kikazi.'***(Al Mughni)*

Ama tunapoangalia mifano ili tufahamu zaidi basi tunaona kua Mutafarraqah hua ni Wajib pia pale itakapokua mavazi ya Imam husika yana Najis ambayo aliyoiona ni Muamuma.Au labda Nguo ya Imam ni Tohara lakini inaonesha Sehemu ya Aura ya Mwili wake katika wakati wa Kurukuu au Kusujudu, kutokana na Ufupi au kutokana na Kutoboka bila ya yeye mwenyewe Imam kujali, na hivyo Maamuma kua ni mwenye kujua kua hapa Imam hana Sala.

Na kwa Mfano wa Sunnah basi hua ni pale Maamuma anapoona kua Imam amewacha Sunnah Ab'adh kwa Makusudi, kwa mfano amewacha kusoma Qunut kwa Makusudi.Au ameiwacha Tahiyyat ya Kwanza ya Sala kwa Makusudi.

Mfano wa Mubah ni kua kwa mfano Imam katika Kusalisha kwake amesoma Kisomo kirefu, au Qunut ndefu au Dhikr Ndefu katika Rukuu au katika Sujud n.k.

Hivyo katika hali kama hii basi Maamuma anaruhusika kuchagua kuendelea na Jamaa kama anaweza na Kama hawezi basi anaruhusika kujitenga na Jamaa hio na hivyo kua ni Mufarraqah. Kwani Mufarraqah hua unaruhusiwa pia katika hali zifuatazo:

Maamuma anapokua anaumwa.

Maamuma anapokua na khofu kua hatoweza kumaliza Jamaa kwa sababu ya Urefu wa Kisomo na yeye kichwa chake kimejaa usingizi.

Maamuma anapokua anahisi jua kuna dharura ya kuenda chooni na kama aiimsubiri Imam amalize basi huenda nae akajimalizia hapo hapo kwenye Sala kwa kutoshindwa kujizuia.

Maamuma anapokua na Khofu ya kupoteza Mali yake.

Inapokua kuna hali ya hatari labda Mtu anataka kuzama,na Maamuma anaweza kumuokoa basi anaruhusika kua Mufarraqah. N.k.

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf an Nawawi kua: '**Haikubaliki kwa Maamuma kua Mufarrah isipokua pale itakapokua kuna dharura, na hivyo inakubalika kuachana na Jamaa kwa dharura ya kutokana na kua Imam anairefusha , pale inapokua Maamuma hawezi kustahmili urefu huo kutokana na Udhaifu wa Kiafya au wa kimajukumu na hii ni kulingana Na Hadith ya Muadh katika Sahihayn'***(Minhaj Talibin)*

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Kama Maamuma ameingia katika Sala ya Jamaa na iisha akaamua kuachana na Jamaa kutokana na Kingizio kinachokubalika kisharia basi hua inaruhusika na hii ni kulingana na Hadith ya Muadh Ibn Jabal ambayo imeelezewa na Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu*isemayo kua:Muadh alisali Sala ya Isha pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhiwa Salam* na kisha akarudi kwa Watu wake na kuwasalisha na akasoma Surat Al Baqara.**

Hivyo mmoja kati ya Maamuma wake akasali peke yake, na Watu wakawa wanamwita Mnafiq Mtu huyo akasema kua yeye si Mnafiq, na nitaenda kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Hivyo akaenda kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumshtakia,na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwita Muadh Ibn Jabal na Kumwambia kua:Unawasababishia watu Mitihani ewe Muadh?

Mara mbili kisha akamwambia: Unaposalisha Watu basi soma Sura *kama Surat Al Buruj, Surat Al Layl, Surat Shams, Sabihisma*.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumwambia Mtu huyo alieachana na Sala ya Jamaa ya Muadh kua hakua na Sala hivyo asali tena, na wala hakumkataza kwa kitendo chake hicho'*(Al Mughni)*

Na pia miongoni mwa mambo yanayoruhusika kwa Maamuma kua Mufarraqah ni pale Imam atakaposahau kukaa Kitako katika Tahiyyat ya Mwisho na Maamuma Wakamkumbusha kwa kusema Subhanah Allah, lakini nae akawa ni mwenye kuendelea na Kisimamo chake.

Yaani kwa mfano baada ya Kumaliza Sujud ya Rakaa ya pili ya Salat Al Fajr basi Imam akanyanyuka na kuja juu na Maamuma akajua kua hii sasa ni Rakaa ya Tatu ambayo haimo kwenye Salat Al Fajr. Au labda kwenye Sala ya Rakaa 3 akanyanyuka kwa Rakaa ya 4, au kwenye Sala ya Rakaa ya 4 akanyanyuka kwa Rakaa ya 5.Basi katika hali kama hii Maamuma hua na haki ya kua Mufarraqah yaani kuachana na Jamaa.

Kwani anasema Imam An Nawawi kua: '**Kama Maamuma atakua na Uhakika wa kua ndio Mwisho wa Sala, basi hua hana ruhusa kunyanyuka na Kumfuata Imam kwa Rakaa ya ziada**. **Na hivyo kama anataka basi anatuhusika kua *Mufarraqah*, akasoma Tahiyyat yake ya mwisho na kutoa Salam, na Sala yake itakua ni Sahii bila ya tatizo lolote**. **Na hii ni kwa sababu yeye ameachana na Jamaa kutokana sababu inayokubalika kishariah**. **Au pia anaweza kubakia hapo hapo chini na kurefusha Dua zake katika Tahiyyat yake hadi Imam atakaporudi kwenye Tahiyyat na kisha kutoa Salam baada ya Salam ya Imam'***(Al Majmuu)*

Na amesema pia Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: **'Wakati Imam anaponyanyuka kwa ajili ya Rakaa ya nyongeza, kwa mfan kama Rakaa ya 5 kutokana na kusahau kwake, basi hua haitruhusiwi kwa Maamua kumfuata Imam katika tukio hilo hata kama Maamuma atakua ni Masbuq(Aliechelewa) au ni mwenye kua na shaka juu ya Idadi ya Rakaa, bila ya kuchukulia**

uwezekano wa kua Imam amewacha moja kati ya Nguzo ya Sala katika Moja kati ya Rakaa. Kwa sababu Jukumu la Maamuma hua ni Kujua nini kinaendelea ndani ya Sala, au kutokana na kua shaka kubwa sana. Basi Maamuma anaweza kua Mufarraqah na kutoa Salam au anaweza kumsubiri Imam arudi kwenye hatua ya kutoa Salam'*(Tuhfah Al Muhtaj)*

Na akasema tena Imam Ibn Hajar Al Haytami kua: **'Ingawa katika hali kama hii inaruhusika kua Mufarraqah lakini hata hivyo hua nibora zaidi kwa Maamuma husika kumsubiri Imam arudi na kutoa Sala kisha na yeye ndio atoe Salam'***(Fatawa Fiqhiyyah Al Kubra)*

Miongoni mwa sababu zinazoruhusika kwa Maamuma kua Mufarraqah ni pale inapokua Imam ameelekea Upande sio wa Kibla.

Au pia Msafiri ambae yuko njiani safarini na anakhofia kua huenda wenzake watamkimbia kama akiendelea na Sala ya Jamaa, iwe safari ya Msafara wa Farasi, Ngamia, Usafiri wa Basi au boti n.k

Basi Msafiri huyu hua anaruhusika kua Mufarraqah, na anaweza akaifupisha Sala yake kwa kuachana na wenzake na akawakimbilia wenzake n.k

Vile vile tusema Maamuma anasali Sala ya Jamaa lakini katika Kusali Kwake akacheua au akatapika, hivyo katika hali kama hii basi Mtu husika hua ni vigumu kwake kuendelea na Sala ya Jamaa na anaruhusika kuachana na Jamaa na kumalizia Sala yake peke yake kisha akaondoka, n.k.

Na pia Mtu anaeumwa na Tumbo labda kwa kukorogeka au mwenye gesi wakati akiwa ndani ya Sala.

Na akahisi kua akiendelea kusubiri kimalizike kisomo kirefu cha Imam itakua balaa, basi hua inaruhusika kwake pia kua Mufarraqah, akamalizia Sala kisha akakimbilia chooni, au Nyumbani n.k.

Na pia kwa Mtu ambae amekula Vitunguu, iwe vitunguu Thoum au Vitunguu Maji au chakula chenye kuta harufu mbaya kwa wenginekama Doriani kwa mfano ambapo kuna baadhi hua wanakirihishwa na harufu yake basi Mtu aliekua vyakulavya aina hizi hua anaruhusika kua Mufarraqah. Kama alivyosema Imam Abd Al Hamid Al Sharwani Al Shafii kua: '**Ni Wajib kwa Mtu yeyote atakaekula kitu kitakachokua na harufu mbaya na kisha akasali Sala ya Jamaa, basi anaruhusika kua Mifarraqah na kuachana na Kumfuata Imam na wala hatoksa malipo ya Sala ya Jamaa, kwani kufanya hivi kwa kila kinachofanana na jambo hili likitokea katika Sala ya Jamaa hua ni bora, kutokana na kuzuia kusababisha Madhara kwa Waumini au kwa Muumini mwenyewe.'***(Hashiyyah Al Sharwani aAla Tuhfah Al Muhtaj)*

Hivyo ingawa Maimam wa Madhhab tofauti wanakubaliana kuhusiana na kuruhusika kwa Maamuma kua Mufarraqah kwa jambo linalokubalika Kisharia ikiwemo Urefushaji wa Qunut.Lakini kwa upande mwengine watu wanaweza kuulizana suali lifuatalo hususan katika Jamii zetu miongoni mwa wengi wale wasiojua kuhusiana na Qunut.

'Kwani tumesema kua kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Qunut ni Sunnan Ab'aadh hivyo ni Wajibu na Mtu akiiwacha basi humbidi kuleta Sijdat Sahw.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik wao wanasema kua Qunut ya Sala Al Fajr ni Mandub lakini kama Mtu akiiwacha au akiisahau basi hua haina haja kwake kuleta Sijdat Sahw na kama Mtu akileta Sijdat Sahw kwa makusudi kwa sababu ya kuisahau Qunut basi Sala yake inabatilika kwa kuongeza ziada ndani ya Sala'*(Hashiyyah Yusuf As Safti Al Maliki)*

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi kaao wanasema kua si Sunnah Kusoma Qunut kwenye Sala ya Al Fajir.

Hivyo Suali linakuja kama ifuatavyo **Jee kwa Anaefuata Madhhab yasemayo kua Qunut Si Sunna anayoruhusa ya kua Mufarraqah yaani kuachana na Jamaa kwa sababu ya kua Imam anasoma Qunut katika Sala ya Alfajir?**

Naam...hili ni suali muhimu sana, kwa sababu katika Jamii yetu kuna wasiojua ambao kutokana na kua wao wanajisifu kua ni wenye kuinusuru Sunna na hivyo wanafuata njia za Vizazi vya mwanzo vya Uislam basi hawawezi kusali katika Miskiti yenye kusomwa Qunut, na hivyo pia wanaruhusika pia kuachana na Jamaa ya Salat Al Fajr na kua Mufarraqah kwa sababu ya Qunut.Hivyo jee inaruhusika kwa Mtu kua Mufarraqah kwa Sababu Imam anasoma Qunuti?

Na ili kupata jawabu la Suali hili basi tunarudi kwa Wanazuoni ambao ni waanzilishi wa haya mambo ya kufuata njia za vizazi vya mwanzo vya Uislam, ambapo kinara wao ni Shaykh Ibn Taymiyyah, ambao wao wenyewe Wanamwita Shaykh ul Islami kutokana na kumkubali kwao.Hivyo anasema Shaykh Ibn Taymiyyah kua:

'Kusoma Qunut katika Salat Al Fajr sio Sunnah, lakini hata hivyo Mtu anaeamini kua ni Sunnah hua ni mwenye kuamini kutokana na Ijtihad (Jithada zake katika Kupata Msimamo sahih wa Kifiqh kutoka katika Vyanzo vyake, yaani Qur'an na Sunnah, Ijmaa na Qiyas). **Basi Ijtihad yake hua inakubalika kama zinavyokubalika Ijtihad juu ya mambo mengine.Kwa maana hio basi Mtu anaefuata Imam katika Sala katika mambo ambayo Ijtihad inakubalika ndani yake**, **anatakiwa amfuate Imam pia katika kila jambo kinalokubalika Ijtihad ndani yake.**

Hivyo Kama Imam akiwa anasoma Qunut katika Sala, basi na yeye Maamuma anaemfuata anatakiwa asome Qunut pamoja nae, na kama Imam akiwa hakusoma Qunut basi na yeye anatakiwa asisome Qunut. **Kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Imam amewekwa kwa ajili ya kufuatwa, na akasema pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Msipingane na Imam wenu.**

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Hadith sahih kua: Maimam wenu wankuongozeni katika Sala zenu, kama wakifanya ndivyo basi Thawabu hua juu yenu na juu yao, na kama wakifanya makosa basi Thawabu hua juu yenu na Dhambi hua juu yao.'*(Al Ikhitiyart)*

Na akasema pia miongoni mwa Maimam wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ambae Imam Mansur Ibn Yunus Al Buhuti kua: '**Amesema Ibn Taymiyah katika Al Ikhtiyarat kua Kama Imam atafanya Jambo ambalo Ijtihad inakubalika ndani yake basi Maamuma anatakiwa amfuate Imam huyo hata kama yeye Maamuma mwenyewe haamini kuhusiana jambo husika kwa mfano Kisomo cha Qunut katika Salat al Fajr.'**

Kwani kwa Maana hio basi kwa wale wanaosema wanainusuru Sunnah na ni wenye kufuata njia za Vizazi vya mwanzo wanatakiwa wajue kua **Hairuhusiki kua Mufarraqah katika Jamaa ya Imam asomae Qunut. Na hivyo pia kama Imam husika atakua ni mwenye kuleta Sijdat Sahw kwa**

sababu kaisahau Qunut katika Salat Al Fajr basi na wewe pia utatakiwa ulete Sijdat Sahw kama kweli ni mwenye Kuinusuru Sunnah au ni mwenye kufuata vizazi vya Mwanzo vya Uislam.

Kwani anasema Muwaffaqah Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Na kama Imam akisahau kitu ndani ya Sala basi na Maamuma amfuate katika Kuleta Sijdat Sahw, iwe Maamuma amesahau ama la**. **Na hii ni kutoka kwa Imam Ibn Al Mundhiri ambae amesema kua Kuna Makubaliano ya Ijmaa ya Wanazuoni wote juu ya hili.'***(Al Mughni)*

Naam..nadhani itakua tumefahamiana, kutokana na kua tuliowanukuu leo ni Maimam wa wanaoinusuru Sunna kwa ajili ya Wanaoinusuru Sunna na wanaofuata vizazi vya awali vya Uislam.

Kwani kuna Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* inayohimiza kila Maamuma kua ni mwenye Kumfuata Imam wake katika Jambo linaloruhusika, kama anavyosema Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu* kua:'**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Kama Mtu akiwa atamfuata Imam wake katika Qiyam tangu mwanzo hadi mwisho basi Sala yake huhesabiwa kama kwamba aliesali Usiku mzima.'** *(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhii, Imam Al Nasai na Imam Ibn Majah)*

Ambapo amesema Imam At Tirmidhii kuhusiana na hadith hii kua **: 'Hii ni Hasan Hadith'**

Hivyo hadith hii inatuonesha umuhimu wa mtu kumfuata Imam katika Ibada ya Sala anapokua Msikitini au anapokua kwenye eneo la Sala ya Jamaa hata kama Imam huyo atakua si wa Madhhab yake au si mwenye kuendana na Mitizamo yake, yaani labda kwa mfano yeye anasoma Qunut na wewe husomi,Au yeye anafunga mikono wewe hufungi, au yeye hafungi na wewe unafunga n.k.

Kwa sababu tofauti hizi hua si sababu zinazokubalika kisharia kwa Maamuma kuachana na Imam au Mtu kuachana na Jamaa wakati yupo ndani ya Msikiti au yuko karibu na Msikiti husika au yuko ndani ya Sala ya jamaa husika.

Na tunapoangalia Suali la Mufarraqah katika Mawsuat*Fiqhiyyah Al Quwaytiyyah* basi tunaona kua nayo inasema kua: '**Mufarraqah hua ni Kitendo kinachoamuliwa na Maamuma katika kuamua Kutomfuata Imam**. **Na kuna tofauti ya Mitizamo juu ya jambo hili miongoni mwa Wanazuoni, kuhusiana na kwamba Sala ya Mtu husika hua inasihi au haisihi**. **Kwani kuna Wanaosema kua Sala hua inasihina Kuna wanaosema kua Sala hua Haisihi kabisaa.'**

'Kuna wanaosema kua Kuna tofauti ya Mtu kua Mufarraqah, kwani hii hua inategemeana na nia ya Mtu, na Nia hua kuna inayokubakika na kuna isiyokubalika. **Hivyo Maamuma anakubalika kua Mufarraqah inapokua Nia yake ni yenye kukubalika, na hua haikubaliki pale nia inapokua haikubaliki.'**

Kwa maana hio basi Mtu anaweza akawa na Nia ya Kusali Jamaa na hivyo akatia nia katika Kusali kwake ya kua yeye anasali Jamaa, na Hivyo ni Maamuma.Lakini sasa kutokana na Dharura inayokubalika Kisharia basi akabadilisha nia ndani ya Sala kua anaachana na Imam na kisha akaendelea kusali peke yake hadi mwisho na kisha akaondoka na hamna tatizo lolote, kwa sababu ya Dharurah yake.

Ila akibadilisha nia ndani ya Sala kutoka kwenye Sala ya Jamaa na kua Mufarraqah bila ya Sababu inayokubalika Kisharia basi Mtu husika hua hana Sala,kwa sababu amejitenga na Imam wake bila ya kua na sababu inayokubalika.Ambapo hapa inabidi tukubaliane kua suali hili hua halimhusu Maamuma ambae ni Masbuq yaani aliechelewa na Kumkuta Imam keshamtangulia katika hatua za Sala.

Na hii ni kwa sababu Masbuq (Mtu aliemkuta Imam ameshamtangulia kwa Rakaa) basi huanza na nia ya Sala ya Jamaa, lakini Imam akitoa salam basi yeye humbidi kunyanyuka na nia ya Kusali peke yake na hivyo hua Mufarraqah mbele ya Imam kwa sababu yeye hua inambidi atimize Rakaa aliyoikosa hapo kabla.

Miongoni mwa sababu zinazopelekea kua ni Wajib kwa Maamuma kua Mufarraqah mbele ya Imam wake ni pamoja pale inapokua Imam anafanya makosa katika Usomaji wa Surat Al Fatiha.Kwani kama tulivyoona hapo awali kua Surat Al Fatiha ni Nguzo ya 4 miongoni mwa Nguzo 13 za Sala.

Hivyo basi kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, basi wanasema kua Haikubaliki kumfuata Imam mwenye Kufanya Makosa katika Usomaji wake wa Surat Al Fatiha pale inapokua kasoro hio ya Kisomo inabadilisha maana ya Aya husika.Na hii ni kwa sababu:

Kwanza Sala yake hua ni Batili, hivyo hua ni Wajibu kwa Maamuma kua Mufarraqah kwa Imam husika.

Na Sababu ya pili ni kua Surat Al Fatiha ni Nguzo ya Sala na hivyo kila Mtu anaesali anatakiwa asome Surat Al Fatiha, akiwemo Imam mwenyewe. Sasa Imam anapokua hawezi kusoma Surat Al Fatiha ipasavyo basi hua hawezi kubeba Jukumu la kufuatwa. Kwa Hivyo Maamuma anawajibika kua Mufarraqah kwa Imam husika

Tatu ni kua Kisharia hua haikubaliki kwa Watu kumchagua Mtu ambae haijui Surat Al Fatiha, kwa sababu kufanya hivyo hua ni kupingana na maamrisho ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam na Allah Subhanah wa Ta'al*a katika Ibada ya Sala kua Imam lazima awe ni mwenye Ilm zaid katika Sehemu Husika.

Na hivyo hii hali ya kupingana na Maarisho ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi waSalam* na *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Ibada ya Sala basi hupelekea Ibada ya Sala husika kua Isiyohesabiwa Malipo yake. Hivyo Maamuma anawajibika Kua Mufarraqah katika Sala hali kama hii. Na hii tunazungumzia pale Imam anapokua anakosea kusoma Surat Al Fatiha na hivyo kubadilisha maana ya aya au za aya.

Lakini pale tunapozungumzia kuhusiana na kukosea kwa Imam Katika Usomaji wake Surat Al Fatiha lakini kukosea kwake huko hua hakubadilishi maana ya Aya husika, basi hapa inakua haipendekezwi kumfuata Imam husika, lakini kumfuata kwake hua hakuipelekei Sala husika inayoongozwa na yeye kubatilika.

Na huu ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Madhab ya Imam Al Shafii, Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik. Na kuna Makubaliano ya Wanazuoni juu ya hili la kua Sala husika hua haibatiliki.

Na hii ni kwa sababu ya kua Imam husika hua ametimiza Wajibu wake wa Kusoma Surat Al Fatiha ndani ya Sala husika. Ila Haipendekezwi kumfuata kwa sababu Imam anatakiwa ni Mwenye Kujua zaidi miongoni mwa watu wa sehemu husika, na kutokana lakini Kasoro ya Kisomo chake basi Imam basi Imam husika hua hana sifa ya kua Imam, labda iwe yeye ndie pekee mwenye kujua zaidi miongoni mwao.

Ama tunpoangalia kuhusiana na mfano wa kuhusiana na pale inapokua ni Haram kwa Maamuma kua Mufarraqah, ambapo tulisema kua miongoni mwa mifano kua ni katika Salat Al Jumaah.

Kwani anasema Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini Al Shafii kua: ‘**Haitakiwi kwa Maamuma kua Mufaraqqah wa Sala ya Jamaa pale anapokua katika Rakaa ya kwanza ya Sala ya Ijumaa**. **Na hii ni kwa sababu Jamaa ya Sala ya Ijumaa hua ni yenye kuhesabika kuanzia katika Rakaa ya kwanza**.

Ama kuhusiana na Rakaa ya pili basi hua haina Ulazima kua ni ya Jamaa na hivyo Katika Rakaa ya pili hua inaruhusika kwa Maamuma kua Mufaraqqah.

Na hii ni tofauti na ilivyoelezewa katika Al Kifayat ambayo imesemwa kua hua hairuhusiki. Hivyo Kama Sala ya Ijumaa utashinidikana Kusaliwa kwa sababu ya Mtu mmoja kua Mufarraqah, basi sisi tunasema kua Sala ya Ijumaa hua ni Fardhu Kifayah, hivyo hua kuna adhabu kwa kuachana nayo. **Kama walivyosema Wanazuoni waliotangulia, kwa sababu Fardh al Kifayah inapokua ni maalum kwa kila Mtu basi hio hua ni Fardh Al Ayn***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Ambapo kabla ya kuendelea basi hapa kwanza inabidi tufahamishane kuhusiana na Hukmu ya Fardh Al Kifayah na Fardh Al Ayn...ambapo:

Fardh Kifayah hua ni Jukumu ambalo linatakiwa kuetekelezwa na Jamii ya Kiislam ya eneo husika au Ummah wa Kiislam kwa Ujumla: Kwa Mfano:Wajibu wa Jamii Kusali Sala ya Ijumaa. Wajibu wa Jamii pale Muislam anapofariki kumkosha kumkosha, Kumkafini, Kumsalia na Kumzika.

Wajibu wa Jamii Kua na Kiongozi, Kusomeshana Dini ya Kiislam, Kua na Madaktari, Kua na Jeshi, Kujenga Miskiti, n.k

Hivyo Fardh Kifaya hua ni Wajib wa Jamii ambao utakapotekelezwa na Baadhi ya Watu katika Jamii basi itatosheleza, lakini kama hakuna wa kuutekeleza basi jamii husika hua ni yenye kufanya Dhambi.

Kwa kila mmoja miongoni mwa Jamii husika kulingana na Uwezo wake.Ambapo Fardh Al Ayn hua ni Jukumu la Kila Mtu kwa mfano Kusali, Kufunga, kutoa Sadaka n.k

Hivyo Tunapozungumzia Sala ya Ijumaa basi tunaona ni Jukumu la Jamii nzima kuanzia kwa kila mmoja miongoni mwa Waislam.

Kwani tunaporudi kwenye Sala ya Ijumaa basi tunaona kua kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni Kua Sala ya Ijumaa huanzia na Idadi ya watu 40.Na kwa kua Hukmu ni hio basi Pale inapokua kuna Watu 40 wanaosali Sala ya Ijumaa basi hua hairuhusiki kwa Mtu yeyote miongoni mwao kuamua kua Mufarraqah anapokua katika Rakaa ya kwanza kwa sababu atakua amepunguza Idadi stahiki ya Watu wanaohitajika ili kuifanya Sala ya Ijumaa ikubalike.

Lakini kama atapatwa na dharura na hivyo kumbidi kua Mufarraqah katika Rakaa ya pili ya Sala ya Ijumaa basi hapa hua inaruhusika, na hii ni kwa sababu kua Mufarraqah kwake katika rakaa ya pili hakuipelekei Sala husika ya Ijumaa kubatilika, kwa sababu ilipoanza ilikua na idadi stahiki ya watu ambao ni 40.

Na hii ni kwa sababu amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Am**esema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Yeyote atakaeiwahi Rakaa ya Sala basi atakua ameiwahi Sala husi**ka*(Bukhari na Muslim)*

Na akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Yeyote atakaieiwahi Rakaa moja ya Ijumaa nyuma ya Imam basi na aongezee Rakaa mo**ja*(Sunan Al Kubra)*

Na akasema tena pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Sala ya Ijumaa ni Wajibu kwa Kila Muislam kwa Jamaa***(Sunan Abu Daud)*

Hapa kuna baadhi wanaweza kua na suali linalouliza: '**Jee Kama Mtu anasali nje ya Msikiti katika Sala ya Ijumaa na ni mwenye Kusikia Sauti ya Imam wake, lakini Ghafla Sauti hio ikakatika baada kukatika kwa Umeme labda, nk.**

Jee Maamuma husika anaruhusika Kua Mufarraqah? Na Jee akiwa Mufarraqah atakua anasali Sala ya Al Jumaa au Adh Dhuhri?

Hivyo ili kujibu suali hili basi kwanza inabidi tufahamiane kua Ili Mtu akubalike kua ni Maamuma basi anatakiwa awe ni mwenye Kujua kuhusiana na Hatua za Sala za Imam wake. Ambapo kujua huko hua kunatokana na Aidha kwa Kumuona Imam au Mtu wa Nyuma yake au kwa Kusikia Sauti ya Imam wake au Sauti ya Mtu alie nyuma yake.

Ambapo hii ni kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: **'Kukubalika kwa Mtu kua Maamuma hua ni kwenye kutokana naKua Maamuma kua ni mwenye kujua kuhusiana na Hatua za Imam iwe wanasali Msikitini au sehemu nyengine yeyote ile, iwe Imam yumo ndani ya Msikiti Maamuma yuko nje n.k.**

Na hili ni Jambo ambalo kuna Makubaliano ya Ijmaa juu yake. **Ambapo As-hab Al Wujuh wetu wanasema kua Maamuma anatakiwa awe ni mwenye kujua hatua za Imam kwa kumsikia au kwa kusikia walio nyuma ya Imam, au kwa kuona kwa Macho yake hatua za Imam au za walio Nyuma yak**e'*(Al Majmuu)*

Ambapo anasema Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini kua: '**Kama ikiwa sauti ya Imam haiwafikii Maamuma, basi baadhi ya Maamuma wanatakiwa watamke kwa Sauti kubwa Hatua za Imam, iwe Maamuma mmoja au zaidi kulingana na hali stahiki.**

Na hii ni kutokana na uthibitisho wa Hadith ya Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam katika Sahihayn pale alipokua akiumwa alisalisha huku Abu Bakr Radhi Allahu Anhu akipaza sauti katika Takbir.'*(Al Mughni)*

Kwa maana hio basi katika hali kama hii kwa Maamuma hua anaweza kua Mufarraqah kama ana sababu inayokubalika.Lakini kama hana sababu basi anatakiwa kusubiri hadi ahakikishe kua hakuna uwezo wa kusikia wala kujua hatua za Imam wake, au pia huenda Umeme ukarudi labda, n.k.

Kwani kwa upande mwengine basi anasema Al Allamah Shaykh ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari Al Shafii katika Asna Matalib kua:**'Na yeyote yule atakaekua Mufarraqah katika Sala ya Ijumaa baada ya kuiwahi Rakaa ya kwanza, basi na amalizie Rakaa ya pili ambayo itamtosheleza kukamilisha Sala yake ya Ijumaa'**

Kwa maana hio basi :Kama Maamuma kwa dharurah inayokubalika ataamua kua Mufarraqah kabla ya kumalizika Rakaa ya kwanza ya Sala ya Ijumaa basi Mtu huyo itambidi asali Sala ya Adh Dhuhr badala yake, yaani amalizie Rakaa 4.'

Kwani vile vile pia kama ikitokea hali kama hio ya kutokua na Mawasiliano baina ya Imam na Maamuma na kisha Maamuma akawa hakuamua kua Mufarraqah, na kisha akaendelea kusali katika hali kama hio na akawa ni mwenye Kumtangulia Imam huku yeye akijua kua ni Maamuma basi Sala yake Itabatilika. Kwa sababu katika Sala ya Jamaa hua hairuhusiki kwa Maamuma kumtangulia Imam.Hivyo katika hali kama hii pia hua inaruhusika kwa Maamuma kua Mufarraqah baada ya kuhakikisha kua hakuna uwezo wa kua na mawasiliano yeyote na Imam.

Ambapo Imam Zakarriyah Al Ansari anaendelea kusema kua: '**Kama Mtu akiamua kua Mufarraqah basi Sala yake inakubalika**.'

'Na kuhusiana na Malipo yake kua ni sawa na Malipo Sala ya Jamaa kwa alieamua kua Mufarraqah basi kwa upande wa Imam Abu Is-haq Al Shirazi na Wanazuoni wengineo basi wao wanasema kua:Mtu anaekua Mufarraqah basi hua ni mwenye kuamua kusali peke yake na hivyo Malipo yake hua ni ya Mtu aliesali peke yake.'

'Na kama Mtu huyo akiamua kubakia na Imam huku akijua kua hakuna mawasiliano baina yao na kisha ikatokea kua akatoa yeye Salam mwanzo kuliko Imam basi Sala ya Mtu huyo hua ni Batili, kwa sababu hua amefanya Makosa mawili, ambayo ni kwanza amemtangulia Imam kwa hatua ya Nguzo ya Sala na kisha Kumuasi Imam kwa kumaliza Sala kabla yake.'

HUKMU YA KUNYANYUA MIKONO KATIKA DUA YA QUNUT

❖❖❖

Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Katika kila Sala ya Asubuhi nilikua nikimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akinyanyua Mikono yake na Kuomba Dua kuwalaani wale waliowaua Masahaba waliohifadhi Qur'an'***(Imam Al Bayhaqi)*

Imam Al Bayhaqi Anaendelea kusema katika hadithi nyengine kua:

عن أبي رافع قال صليت خلف عمر بن الخطاب رضى الله تعالى عنه فقنت بعد الركوع ورفع يديه وجهر بالدعاء

Amesema Abu Rafiu kua:'Nilisali Mimi nyuma ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na alikua akisoma Qunut huku akusa ni mwenye Kunyanyua juu Mikono yake yote miwili na Sauti yake.'*(Imam Al Bayhaqi)*

Na akasema Salman Al Farisi *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

Hakika ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Alie Hai na ni Mkarimu Sana kiasi ya kua pale Mja wake anaponyanyua Juu mikono yake kumuelekea yeye. *(Allah Subhanah wa Ta'ala* kumuomba) basi *(Allah Subhanah wa Ta'ala)* hua ni mwenye Kuona Haya sana kwa Mja huyo Kuirudisha Mikono yake ikiwa mitupu bila kujibiwa'*(Imam At Tirmidhi)*

Naam..Hizi ni baadhi ya Hadith ze ye kuthibitisha mambo mawili, ambapo la kwanza ni Kuhusiana na Sunnah ya Kunyanyua Mikono na kuelekeza Juu viganja vya Mikono katika wakati wa Kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Pili ni kuhusiana na Sunnah ya Kunyanyua Mikono na kuelekeza viganja juu katika wakati wa Kisomo cha Qunut ndani ya Sala.

Kwani Ingawa kuhusiana na Mtizamo wa Imam Al Qaffal Al Shashi Al Marwazi Al Shafii,Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii na Imam Al Baghawi Al Shafii tunaona kua wao wanasema kua;

'Sio Lazima Kunyanyua Mikono Juu katika Wakati wa Kuomba Dua ya Qunut ndani ya Sala, na hii ni kwa sababu Dua ya Qunut hua ni sawa na Dua inayosomwa katika Wakati Mtu anapokua katika Sujud ya Sala, na pia ni sawa na ile inayosomwa katika Tahiyyat ya Mwisho ndani ya Sala ambayo Mikono hua hainyanyuliwi ndani yake.'

Lakini kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi yeye anasema kua: '**Hua ni Sunna kwa Mtu anaesali kunyayua mikono yake katika Wakati wa kusoma Qunut**

Na huu ndio Mtizamo unaokubalika zaidi miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, kulingana na Vithibitisho vya Hadith kama alivyonukuu Imam Al Bayhaqi katika Hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambayo ni Hadith Hasan Sahih inayoelezea Watu wa Mji wa Qura waliouliwa.'

Naam..anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Na Qunut hua ni Sunnah pale Mtu anapoinuka kutoka katika Rukuu ya Rakaa ya pili ya Salat Al Fajr**. **Na kinachosemwa hua ni *Allahuma Ihdina Fii man Hadayt.*.hadi mwisho wa Dua hio.**

Ambapo Imam hua anasoma katika Hali ya Wingi na kile kilichokua Sahih katika Fua hio ni kua hua ni **Sunnah pia ndani yake kumtumia *Salam Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*mwishoni mwa Dua hio.Na Mikono Hunyanyuliwa Juu na haitakiwi kupangusa Uso baada ya Kumaliza Na Imam anaposoma Husoma kwa Sauti huku wale Wanaofuata Huitikia Aamiin.'***(Al Minhaj Bi Sharh Sahih Muslim).***

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Naqib basi yeye anasema katika Umdat Salik wa Udat An Nasik kua: '**Katika Kusali Sala ya Alfajr hua ni Sunnah kunyanyua Mikono na Kuomba Dua ya Qunut baada ya Kusimama kutoka katika Rukuu ya Rakaa ya pili ambapo Mtu hua anasema: Allahuma Ihdini fii man Hadayt, Waafini fii man Afayt....'**

Imam Ibn Naqib Al Misri anaendelea kusema kua: '**Baada ya Kisomo Mtu hua Hapangusi Uso wake wala Kifua chake.'**

Na Ingawa hua ni Sunnah Kupangusa mikono kwenye Uso baada ya kuomba Dua kama alivvyosema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:Wakati mnapoomba Dua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Ombeni kwa Matumbo ya Viganja vyenu na wala sio Nyuma yake, na mara mtakapo maliza basi panguseni Nyuso zenu kutokana nayo**.'*(Imam Abu Daud,Imam Ibn Majah, Imam Al Hakim)*

Na amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua:

كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا رَفَعَ يَدَيْهِ فِي الدُّعَاءِ لَمْ يَحُطَّهُمَا حَتَّى يمسح بهما وَجهه. رَوَاهُ التِّرْمِذِيّ

‘**Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akinyanyua mikono yake kwenye Dua basi alikua hairudishi hadi ajipangusie Uson**i.*’(Imam At Tirmidhii)*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani kuhusiana na Hadith hizi kua: ‘**Hadith hii (Ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu)* inaungwa mkono na na hadith nyenginezo ikiwemo hadith ya Abd Allah Ibn Abbas aliyoinikuu Imam Abu Daud na kwa pamoja zinaashiria kua ni Hadith zenye sifa ya Hasan Hadit**h’*(Bulugh Al Marami)*

حَدَّثَنَا قُتَيْبَةُ بْنُ سَعِيدٍ، حَدَّثَنَا الْمُفَضَّلُ، عَنْ عُقَيْلٍ، عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، عَنْ عُرْوَةَ، عَنْ عَائِشَةَ، أَنَّ النَّبِيَّ قُلْ هُوَ }صلى الله عليه وسلم كَانَ إِذَا أَوَى إِلَى فِرَاشِهِ كُلَّ لَيْلَةٍ جَمَعَ كَفَّيْهِ ثُمَّ نَفَثَ فِيهِمَا فَقَرَأَ فِيهِمَا ثُمَّ يَمْسَحُ بِهِمَا مَا اسْتَطَاعَ مِنْ جَسَدِهِ {قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ} وَ{قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ} وَ{اللَّهُ أَحَدٌ يَبْدَأُ بِهِمَا عَلَى رَأْسِهِ وَوَجْهِهِ وَمَا أَقْبَلَ مِنْ جَسَدِهِ يَفْعَلُ ذَلِكَ ثَلاَثَ مَرَّاتٍ.

‘Na amesema Qutaybah Ibn Said kua amesema Mufadhalu kua amesema U’qayl kua amesema Ibn Shihab kua amesema Aruwat kua amesema Aisha R*adhi Allahu Anh*a kua:‘Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akienda Kulala kila Siku alikua akiweka pamoja viganja vyake, kisha huvipulizia, na kusomea Surat Al Ikhals, Surat Al Falaq, na Surat An Nas na kisha Hujipangusia katika sehemu awezayo ya mwili wake kwa kuanzia Kichwani, Usoni na sehemu za mbele za mwili wake, kwa kufanya hivyo mara tatu’*(Bukhari na Muslim)*

Na amesema Yazid Ibn Said Ibn Thamamah *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘**Kila wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akiomba Dua basi Hunyanyua Juu mikoni yake na kisha hupangusia Uso wake kwa mikono yake hio.’***(Musnad Imam Ahmad)*

Na akasema Abu Nuaym kua: ‘**Mimi nimemuona Umar na Ibn Zubayr wakiomba Dua na kisha kupangusia Nyuso zao kwa Viganja vyao’***(Adab Al Mufrad - Imam Al Bukhari)*

Na akasema Mujaddid Ad Din Imam Jalal Ad Din Al Suyuti kua: ‘**Hasan Al Basr alikua ni mwenye kupangusa Uso wake pia kwa viganja vyake baada ya kuomba Dua’***(Fad Al Wiaa)*

Naam..hivyo ingawa kupangusa uso baada ya kumaliza kusoma Dua hua ni Sunnah lakini hii hua ni nje ya Sala, na si ndani ya Sala na huu ndio mtizamo unaokubalika zaid katika Madhhab ya Imam Al Shafii.

Kwani anasema Imam Al Bayhaqi katika Sunnah Al Kubra kua: ‘**Ama kuhusiana na Kupangusia Uso mara baada ya kumalizia kuomba Dua, basi haikuwahi kunukiliwa kutoka katika vizazi vya mwanzo, katika Qunut, bali imenukuliwa na baadhi yao baada ya kuomba Dua Nje ya Sala’***(Sunan Al Kubra)*

Na akasema Imam An Nawawi kua: ‘**Ama kuhusiana na kupangusia Usoni baada ya kumaliza kuomba Dua ya Qunut,kama tukisema kua Mtu hanyanyui mikono,basi Kupangusia Uso hua**

hakuna na hii ni bila ya kutokukubaliana juu yake. **Na kama tukisema kua Mtu ananyanyua Mikono basi juu yake hua kuna mitizamo miwili ambapo Mtizamo mashhuri.**

Basi hua ni kua inapendekezwa na miongoni mwa waliosimamia Mtizamo huu ni Al Qadhi Abu Tayyib Al Tabari, Imam Abu Muhammad Al Juwayni na Imam Al Ghazali.Ambapo Mtizamo wa pili ni kua haitakiwi kupangusia Uso ndani ya Sala baada ya Qunut, na huu ndio Mtizamo uliokua sahih na ulithibitishwa na Imam Al Bayhaqi, Imam Al Rafii na Wanazuoji wengineo.'*(Al Majmuu)*

Kwani hapa katika kauli ya Imam An Nawawi tunaona kua ametaja Mtizamo Mashhuri, na tunapozungumzia Mtizamo Mashhuri yaani *Qawl Al Mashhur* basi hua haimaanishi kua Mtizamo Unokubalika zaidi, yaani *Qawl Al Mutammad* ambao hua ndio Mtizamo Mkuu wa Madhhab.

Kwani *Qawl Mashhur* hua ni Mtizamo unaojulikana na wengi kua upo Mtizamo huo, lakini si wenye kua na nguvu yaani Mtizamo dhaifu kwa sababu wengi miongoni mwa Wanazuoni wamepingana nao.

Hivyo Mtizamo huo maarufu ambao ni wenye kusema kua Inapendekezwa kupangusia Uso katika Dua ya Qunut ni mtizamo pia wa Imam Ibn Sabbagh Al Shafii, Imam Al Mutawwali na Imam Nasr Al Shafii ambae ni mwandishi wa Kitab Al Bayan.

Ambapo hii pia inaonesha kua ni Sunna kupangusia Uso kwa matumbo ya viganja vya mikono baada ya Kuomba Dua.

Ama kwa upande mwengine basi kuhusiana na Kunyanyua Mikono katika Kuomba Dua Ndani ya Sala basi amesema pia Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:

كان النبي صلى الله عليه وسلم لا يرفع يديه في شيء من دعائه إلا في الاستسقاء وإنه يرفع حتى يرى بياض إبطيه

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua hanyanyui mikono yake kuomba katika Dua yeyote isipokua katika Salat Al Istiqsa. Na anapofanya hivyo alikua akinyanyua mikono yake kiasi ya kua weupe wa kwapa zake ulikua ukionekana.'(Sahih Bukhari)*

Ambapo Salat Al Istiqsa hua ni Sala ya Kuomba Mvua.Na anasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani kuhusiana na Hadith hii kua: '**Kikichobainishwa na Hadith hii ni Kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakunyanyua Mikono katika kuomba kwake Dua isipokua katika Al Istiqsaa, Ambapo jambo hili linapingana na Hadith nyingi sana nyenginezo ambazo ni zenye kusema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akinyanyua mikono katika Kuomba Dua.**

Hivyo inawezekana ikawa ni kweli Anas Ibn Malik Radhi Allahu Anhu alimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akifanya hivyo mara moja tu, na hivyo wale waliomuona akifanya hivyo zaidi ya mara moja kua ni wenye kumtangulia Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu.*

Na pia inawezekana ikawa maneno ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* yanamaanisha kua hakuwahi yeye kumuona akinyanyua mikono juu zaidi kama kwenye Dua ya kuomba Mvua isipokua mara hio Moja tu. **Kiasi ya kua hadi weupe wa kwapa zake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ukawa ni wenye kuonekana.'***(Fath Al Barr)*. Hivyo huo ndio Ufafanuzi wa Imam Ibn Hajar Al Asqallani kuhusiana na Hadith hii.

Kwani tunaporudi katika kupangusa uso kwa viganja vya mikono baada ya kuomba Dua.Basi anasema Imam Abd Razzaq Al Sanan ambae ni Muandishi wa Kitabu cha Hadith cha Musanaf Ibn Abd Razzaq anasema kua: '**Amesema Imam Ma'mar, kua amesema Imam Az Zuhri kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akinyanyua mikono yake katika wakati wa kuomba Dua na kisha Hujipangusia kwenye Uso wake Mtukufu**. **Na mimi nimemuona Mwalimu wangu Imam Ma'mar akifanya hivyo, hivyo na mimi hufanya hivyo.'***(Musannaf Abd Razzaq)*

Na akasema Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari katika Asna Matalib kua: '**Amesema Imam An Nawawi katika Tahqiq kua Inapendekezwa Kupangusa Uso kwa Viganja baada ya kuomba Dua.'**

Ambapo maneno hayo hayo pia ameyasema Imam Al Khatib Al Shirbini katika Al Mughni Al Muhtaj. Na tunaporudi kwa Imam An Nawawi mwenyewe basi amesema tena katika Al Adhkar kua: '**Miongoni mwa adabu za Kutafuta Baraka za Dua hua ni Kuelekea Kibla, Kunyanyua Mikono**, **Kupangusia Uso baada ya Kuomba na Kuifanya Sauti kua ya chini lakini ni yenye kusikikana.'***(Al Majmuu)*

Na akasema Imam Ali Al Shurnbulali Al Hanafi kua: **'Muislam Anatakiwa kumalizia Dua kwa Kusoma aya ya Qur'an isemayo: Subhana Rabbika Al Izzati aAmaa Yasifuuna na hii ni kulingana na Kauli ya Imam Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua Yeyote anaetaka kupata Faida kamili kimalipo katika Siku ya Malipo basi mwache. Na Afanye maneno yake ya Mwisho katika Dua yawe Subhana Rabbika Al Aizzata Aamaa Yasufuuna, na kisha apangusie Uso wake kwa Viganja vyake***(Durar Al Hukam)*

Ambapo maneno hayo ni maneno ya aya ya 180ya Surat As Saffat hivyo wengi hua ni wenye kumalizia kwa aya tatu za mwisho za Sura hio zisemazo:

﴿سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ ٱلْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ ۞ وَسَلَامٌ عَلَى ٱلْمُرْسَلِينَ ۞ وَٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَالَمِينَ﴾

Subhana rabbika rabbi alAAizzati AAamma yasifoona ; Wasalamun AAala almursaleena; Waalhamdu lillahi rabbi alAAalameena*(Surat Saffat 37:180-182)*

*Tafsir: U**tukufu ni wa Mola wako Mola wa mwenye Utukufu na Uwezo wa juu kabisa ambae yuko mali na wanayomsifia, na sala ziwafikie Mitume na Shukran izote anastahiki Mola wa Ulimwengu, na kila kilichomo ndani yake.***

Na akasema Imam Al Nafrawi Al Maliki kua: '**Inapendekezwa kupangusa Uso kwa viganja vya mikono baada ya kuomba Dua kwani ni katika kufuaga Sunnah ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.'(***Fawakih Al Dawani)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Buhuti Al Hanbali basi yeye amesema kua: '**Muislam anatakiwa kupangusia Uso wake kwa viganja vyake baada ya Qunut ndani ya Sala na nje ya Sala kama ataomba Dua.'***(Sharh Al Muntaha Al Iradat)*

Na ingawa Sultan Al Ulamaa Imam Al Izz Ibn Abd Salam amesema kua: **'Ni Mtu mjinga tu ndie anaepangusa Uso baada ya kuomba Dua.'**

Lakini kwa Upande wa Al Allamah, Al Faqih Shaykh Ul Islami Imam Abu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Bahadir Al Zarkashi Al Shafii basi amesema kuhusiana na kauli hio ya

Imam Izz Ad Din Ibn Abd Salaam kua: '**Mtizamo wa Al Izz Ad Din Ibn Abd Salaam ambao ameuelezea katika Fatwa zake kuhusiana na Kupangusa Uso baada ya kuomba Dua kua ni jambo linalofanywa na Wajinga basi inaonesha kua yeye hakuzisoma Hadith zinazohusiana na Jambo hili.Kwani mbali ya kua baadhi wanasema kua Sanad zake ni Dhaifu lakini ni zenye kua na nguvu kutokana na Vyanzo tofauti vya Sanad zake katika Kunukuliwa.'** *(Azhiya fi Al Addiyah)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Is-haq Ibn Rahawayh basi yeye anasema kua: **Ameniambia mimi Mutamir Ibn Sulaiman kua amemuona Abu Kaab ambae ni mwandishi wa Al Harir akinyanyua Mikono yake katika wakati wa kuomba Dua na kisha akajipangusia Usoni, hivyo akamuuliza: Umemuona nani akifanya hivyo? ambapo nae akasema: Al Hasan Abu Al Hasan (Hasan Al Basr)***(Faad Al Wuaah)*

Hivyo wengi Sana miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Malik, Imam Al Shafii na Imam Hanbal wanakubaliana kua inaruhusika kupangusa Uso kwa Viganja vya mikono baada ya Kuomba Dua pale inapokua Nje ya Sala. Kama alivyosema Imam An Nawawi, Imam Al Zarkashi, Imam Al Suyuti, Imam Al Mardawi n.k.

Na pia ndivyo alivyosema Imam Al Haskafi Al Hanafi kua:' **Na kupangusa Uso Baada ya Dua hua ni Sunn kulingana na Mtizamo Uliosahihi kabis**a'*(Durr Al Mandhur)*

Na kama ilivyoandikwa kwenye Fatawa Alamgiri ambacho ni Kitabu maarufu cha Fatwa za Madhhab ya Imam Abu Hanifa kinachojulikana pia kama Fatawa Al Hindiya kua: '**Kupangusa Uso kwa mikono baada ya Muombaji Dua kumaliza kuomba Dua ni kitu ambacho ni Sahih na wengi miongoni mwa Mashaylh zetu Allah awarehemu ni wenye kufanya hivyo na kuna Hadith juu yake.'**

Na kama alivyosema Imam Al Mardawi al Hanbali kua: '**Kuna Mitizamo miwili kuhusiana na kupangusa Uso, baada ya kuomba Dua ambapo mmoja ni kua inaruhusika kupangusa Uso baada ya kuomba Duana hivyo ndigyo alivyokua akifanya Imam Ahmad Ibn Hanbal.Na kama alivyosema Al Majd katika Sharh yake na pia Muandiahi wa Majma Al Bahrain, na pia katika Al Kafi na hivyo ndivyo itakiwavyo zaid kam ilivyoelezewa katika Al Wajiz pia.'***(Al Insaaf)*

Ama kuhusiana na Kufanya hivyo ndani ya Sala baada ya Kumaliza kusoma Qunut basi kuna waliosema kua inafaa akiwemo Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali na Mwalimu wake Imam Al Ghazali pia ambae ni Imam Abu Muhammad Al Juwayni Al Haramayn. Ambayo hio tulisema kua ni *Qawl Al Mashhur* au Kauli Maarufu kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo kwa upande mwengine basi baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal pia wanasema kua Inakubalika kupangusa Uso ndani ya Sala baada ya Qunut.Lakini mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kua Haikubaliki Kupangusa Uso ndani ya Sala baada ya Sala ya Qunut.

Hivyo Wanazuoni Wanakubaliana kua Inapendekezwa kupangusa Uso kwa viganja vya Mikono baada ya Kuomba Dua nje ya Sala.Na wametofautiana kuhusiana na Kuiubalika kupangusa Uso baada ya Kuomba Dua ya Qunut ndani ya Sala kwani wengi, kwani Mtizamo wa wengi ni kua Haifai.

Naa kabla ya kuendelea basi kuna Suali limejitokeza ambalo linauliza: '**Kama Qunut hua ni Dua na katika Fua hua tunaitikia Amiin, jee katika wakati wa Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salaam* mwishoni mwa Dua ya Qunut tunatakiwa tuitikie vipi?'**

Naam.Jibu la Suaki hili analo Shaykh Ul Islami Imam Abu Yahya Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Shafii ambae anasema katika Asna Matalib kua: '**Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani ya Qunut ya Sala hua ni Dua pia na hivyo Imam anapomsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Maamuma anatakiwa kuitikia Amiin.'**

Na kuna Suali Jengine Mtu anaweza kujiuliza kwa kusema kua Mimi ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii hivyo Qunut kwangu ni Wajib lakini Nasali katika Msikiti ambao si wa wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, na hivyo Al Fajir haisomwi Qunut ndani yake, Jee afanyeje?

Hivyo anasema Imam Muhammad Al Zuhayli Al Shafii kua: '**Miongoni mwa Masharti ya Maamuma Kumfuata Imam, basi ni Kua Maamuma kua hatakiwi kuamini kua Sala ya Imam husika haikubaliki kwa sababu akiamini hivyo basi Sala yake yeye hua ni Batili. Hivyo kama Mtu ni mwenye kufuata Madhhab ya Imam Al Shafii akaingia Msikitini akakutana na Imam anaryia Udhu na anaesalisha kulingana na Madhhab ya Imam Abu Hanifa**. **Na kisha mtu huyo Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii akafikiria kua Sala inayosalishwa naImam wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua haifai, basi Maamuzi yake ya kumfuata Imam huyo hua ni yenye kubatilisha Sala yake hio.'**

'Na hii ni kutokana na Mtizamo wake wa Kudhania kua Imam wake Hana Sala. **Hivyo Maamuma anatakiwa aamini kua Sala ya Imam wake ni Sahih mbali ya kua wanatofautiana Kimadhehebu kunakotokana na utofauti wa Mambo madogo madogo ya Jitihada za Kiilm na kimtizamo'***(Al Mutammad Fi Al Fiqh Al Shafii)*

Ama kuhusiana na Qunuti basi anasema mwanafunzi wa Imam Zakarriyah Al Ansari ambae ni Imam Al Shafii Al Saghir Al Faqih Shaykh Ul Islami Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Manugi Al Misri Shams Ad Din Al Ramli Al Shafii kua: ' **Kama mtu ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii katika Sala ya Alfajir akaingia Msikitini ambao ndani yake anasalisha Imam wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa**. **Basi kama Imam atasoma Qunut na kisha Maamuma akamuwahi na Kuenda nae pamoja kwenye Sujud katika Rakaa yake ya kwanza, basi Mtu huyo anaweza kuenda nae Imam huyo.'**

'Na kama Imam hakusoma Qunut basi na yeye haruhusiki kusoma Qunut lakini atatakiwa kuleta Sijda Sahw mwishoni mwa Sala kwa nia ya kua Imam amesahau kusoma Qunut. **Na hii hua ni tofauti pale inapokua Maamuma kamkumbusha Imam kua anatakiwa asome Qunut lakini hata hivyo Imam husika hakusoma Qunut, ambapo katika hali kama hii basi Maamuma hatowajibika Kuleta Sijdat Sahw, kwa sababu haikuachwa na Imam kutokana na Kusahauliwa.'**

'Hivyo Maamuma hatowajibika Kuleta Sijdat Sahw kwa sababu Imam ameiwacha Qunut wakati Maamuma tayari alishaiomba isomwe Qunut hapo kabla,na ukweli ni kua hiruhusiki kwa Maamuma kuleta Sijda Sahw Kutokana na hali hii ya kimazingira' *(Nihayat Al Muhtaj)*

Ambapo hivi pia ndivyo alivyosema Imam An Nawawi katika Rawda Talibin kua: '**Kama Maamuma wa Madhhab ya Imam Al Shafii akimfuata Imam wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, na Kisha Imam akasita kidogo baada ya Kunyanyuka kutoka katika Rukuu ya pili kumuachia Maamuma asome Qunut. Basi Maamuma wa Madhhab ya Imam Al Shafii anaruhusika kusoma Qunut**. **Lakini kama Imam hakufanya hivyo bali kaendamoja kwa moja kwenye Sujud basi na Maamuma itambidi amfuate Imam kwenye Sujud.'**

‘Hivyo Kama Imam alisita kumpa nafasi Maamuma asome Qunut lakini Maamuma hakusoma basi Maamuma itambidi alete Sijda Sahw, kwa sababu ni kosa lake.Lakini kama ikiwa kosa ni la Imam kua hakutoa nafasi hio basi Maamuma haruhusiki kuleta Sijda Sahw.’

‘Na kama Mfuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa anamfuata Imam wa Madhhab ya Imam Al Shafii katika Sala ya Al Fajr, na kisha Imam akaleta Sijdat Sahw kwa sababu aliisahau Qunut basi na Maamuma anatakiwa amfuate Imam kwenye Sijda Sahw.’

‘Lakini kama Imam hakuleta Sijdat Sahw, basi Maamuma hua hana wajibu wa kuleta Sijda Sahw.’

QUNUT – KATIKA SALAT AL WITR YA MWEZI WA RAMADHAN.

❖❖❖

Imetajwa katika Ruhu'l-Bayan kua: ***‘Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **aliwasalisha Mitume wote katika Masjid Al Aqsa Sala ya Sunna ya Rakaa mbili katika Usiku wa Miraj. Na alipokutana na Nabii Musa Mbinguni basi Nabii Musa *Alayhi Salam* alimuomba *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amsalie Sala ya Rakaa moja ya Witr katika Sidrat Al Muntaha.**’*(Ruh Al Bayan)*

Naam..hio ndio asili ya Salat Al Witr Rakaa moja. Anasema Shaykh Ul Islami Imam Ahu Zakarriyah Yahya Ibn Sharraf An Nawawi A Shafii kua: ‘***As-hab Al Wujuh*** **(Wanazuoni Wakuu wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii) wetu wamesema kua:Inapendekezwa Kusoma Qunut kuanzia Katikati ya Mwezi wa Ramadhan katika Rakaa ya mwisho ya Sala ya Witri.**

Na hii ni kutokana na Hadith iliyonukuliwa na Imam Abu Daud ambae amesema kua:

عن الحسن أن عمر بن الخطاب جمع الناس على أبي بن كعب، فكان يصلي لهم عشرين ليله، لا يقنت بهم إلا في النصف الباقي، فإذا كانت العشر الأواخر تخلف فصلى في بيته فكانوا يقولون: أبق أبي.

‘**Amesema Hasan Al Basr kua: Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* aliwakusanya Watu Nyuma ya Ubbay Ibn Qaab *Radhi Allahu Anhu,* ambae akawasalisha kwa mda wa siku 20.Ambapo alikua hasomi Qunut pamoja nao isipokua katika Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan. Na ilipokua zimebakia Siku 10 za 10 la mwisho basi alikua akisali Nyumbani kwake. Na hivyo Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakawa wanasema kua Ubbay amewakimbia**.’*(Al Majmuu)*

Ambapo anasema Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki kua: ‘**Kisingizio cha Ubbay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* kuamua kusali nyumbani kwake katika siku 10 hizo za mwisho wa mwezi wa Ramadhani ambazo ndio bora zaidi ni kua alikua ni mwenye kutaka kuupata ukaribu wa upekee baina yake na *Allah Subhanah wa Ta’ala* ambao ilikua ni vigumu kuupata pale alipokua na Waumini wenzake’**.*(Al Miraqaat)*

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Al Mundhiri basi yeye amesema kua: ‘**Al Hasan Al Basr alizaliwa katika kipindi cha wakati wa utawala wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* mnamo**

mwaka 21 Al Hijr ambapo Umar *Radhi Allahu Anhu* alifariki mwishoni mwa mwaka 23 Al Hijra namwanzoni mwa mwaka 24 Al Hijra.'

Imam Al Zaylai anasema kua: **'Sanad ya Riwaya hii imekatishwa, kwani Hasan Al Basr hakuwahi kukutana na Umar, na Imam An Nawawi mwenyewe amesema katika Al Khulasa kuhusiana na Hadith hii kua ni dhaif. Ibn Abd amenukuu kutokakwa Al Kamil kuiptia kwa Abu Atiqa kupitia kwa Anas *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*alikua akisoma Qunut katika nusu ya mwishoni mwa Mwezi wa Ramadhani'na Abu Atiqa ni dhaif.'**

Na Imam Muhammad Ibn Nasr Al Marwazi amesema kua kitabu chake cha Qiyam Al Layl kua: **'Ama kuhusiana na Qunut katika Salat Al Witr ya Mwezi wa Ramadhani basi amesema Al Hasan kua, Ubbay Ibn Kaa'b *Radhi Allahu Anhu* aliwaongoza Watu katika Sala ndani ya mwezi wa Ramadhani na hakuwahi kusoma Qunut katika Nusu ya kwanza ya mwezi wa Ramadhani bali alisoma katika nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhani, na zilipowadia siku 10 za mwisho wa mwezi wa Ramadhani akakimbia na kuwaacha watu hao, na hivyo Muadh Al Qarri akawa ndie anaewaongoza katika Sala.'**

Na Imam Said Ibn Jubayr aliulizwa kuhusiana na mwanzoni mwa Qunut katika Salat Al Witr hivyo akasema: **'Umar Ibn Al Khattab alituma Jeshi ambalo lilifanya makosa, na hivyo akwa na khofu juu yao, hivyo ilivyoingia Nusu ya pili ya Ramadhani akaanza kusoma Qunut kwa ajili ya kuwaombea.'**

Ambapo kwa upande mwengine basi kama tulivyoona hapo awali katika Hadith kua: '**Amesema Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu kua: Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Dua ya Qunut Mwishoni mwa Sala yake ya Witr kama ilivyoelezewa na Imam At Tirmidhii'**

Na akasema pia Imam Muhammad Ibn Nasir kua: '**Amesema Muhammad Ibn Rafi kua amesema Abd Razzaq kua amesema Ibn Jurayj kua amesema Muhammad Ibn Ali kua amesema Abd AllahIbn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Qunut katika Salat Al Fajr na katika Salat Witr katika wakati wa Usiku**.*'(Mukhtasar Qiyam Al Layl wa Ramadhan)*

Na akasema Imam Ibn Jurayj kua amesemaAbd Rahman Ibn Hurmuz kua amesema Muhammad Ibn Hanafiyyah kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Qunut katika Salat Al Fajt n kwenye Sala ya Witr ya Usiku kwa maneno yasemayo**: ***Allahuma Ihdini fii man hadayt...****(Imam Al Bayhaqi, Imam Abd Razzaq,Imam Ibn Hajar Al Asqallahi katika Talkhis)*

Kwami anasema Al Aswad kua: '**Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* alikuakila anapomaliza Rakaa ya Tatu ya Salat Al Witr basi alikua akisoma Qunu**t' (*Musanaf Ibn Abi Shaybah)*

Na anasema Imam Abu Hanifa kua**: 'Amesema Hamad Ibn Ibn Abu Sulayma kua amesema Ibrahim An Nakhai kua:Qunut ni Wajib katika Salat Al Witr ya Mwezi wa Ramadhan na Nje yake na hua kabla ya Kurukuu na baada ya kumaliza Qunut basi unasema Allahu Akbar kisha unarukuu.'***(Kitab Al Hujjah)*

Naam..huo ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kuhusiana na Qunut katika Salat Al Witr iwe ndani ya mwezi wa Ramadhan au nje yake.Ambapo kwa upande wa Madhhab yao basi pia wao hua Wanasali Salat Al Witr kama inavyosaliwa Salat Al Maghrib.Yaani Rakaa Tatu kwa pamoja, na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: '**Yeyote anaetaka Kusali Salat Al Witr kama Rakaa tatu kwa pamoja basi na Asali.'***(Sunnan Abu Daud)*

Na piakutokana na kua amesema Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Sala ya Witr hua ni Rakaa Tatu za Sala ya Jioni yaani Salat Al Maghrib.'***(Imam At Tahawi, Sharh Al Maani Al Athar)*

Na amesema Aisha *Radhi Allahu Anh*a kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Rakaa Nne za Tahajjud, na msiulize juu ya Urefu wake Rakaa hizo. Kisha alikua akisali Rakaa nne na msiulize juu ya Urefu wake,na kisha alikua akisali Rakaa Tatu.'***(Bukhari na Muslim)*

Na kuna Hadith isemayo kua:

أَخْبَرَنَا يَحْيَى بْنُ مُوسَى، قَالَ: أَنْبَأَنَا عَبْدُ الْعَزِيزِ بْنُ خَالِدٍ، قَالَ: حَدَّثَنَا سَعِيدُ بْنُ أَبِي عَرُوبَةَ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ عَزْرَةَ، عَنْ سَعِيدِ بْنِ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبْزَى، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ أُبَيِّ بْنِ كَعْبٍ قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ فِي الْوِتْرِ بِسَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى، وَفِي الرَّكْعَةِ الثَّانِيَةِ بِقُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ، وَفِي الثَّالِثَةِ بِقُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ، وَلَا يُسَلِّمُ إِلَّا فِي آخِرِهِنَّ، وَيَقُولُ ـ يَعْنِي بَعْدَ التَّسْلِيمِ ـ: «سُبْحَانَ الْمَلِكِ الْقُدُّوسِ»، ثَلَاثًا

Amesema Yahya Ibn Musa kua amesema Ameniambia Abd Al Azizi Ibn Khalid kua amesema Said Ibn Abi Arubata kua amesema Qatada kua amesema Azrata kua amesema Abd Rahman Ibn Abza kua amesema Baba Yake kua Ubbay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* amesema kua:

***'Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* alikua akisoma katika Witr, *Sabihsma Rabika al Aala Qul Yaa Ayyuha Al Kafiruun* na *Qul Huwwa Allahu Aahad* na alikua hatoi salam isipokua katika Rakaa ya mwisho ambapo baada ya *Taslim, Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* husema *Subhanah wa Maliki Al Quddus* mara tatu'**

Na amesema Imam Abu Daud kua

حَدَّثَنَا أَحْمَدُ بْنُ صَالِحٍ، وَمُحَمَّدُ بْنُ سَلَمَةَ الْمُرَادِيُّ، قَالاَ حَدَّثَنَا ابْنُ وَهْبٍ، عَنْ مُعَاوِيَةَ بْنِ صَالِحٍ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي قَيْسٍ، قَالَ قُلْتُ لِعَائِشَةَ رضى الله عنها : بِكَمْ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يُوتِرُ قَالَتْ : كَانَ يُوتِرُ بِأَرْبَعٍ وَثَلاَثٍ، وَسِتٍّ وَثَلاَثٍ، وَثَمَانٍ وَثَلاَثٍ، وَعَشْرٍ وَثَلاَثٍ، وَلَمْ يَكُنْ يُوتِرُ بِأَنْقَصَ مِنْ سَبْعٍ، وَلاَ بِأَكْثَرَ مِنْ ثَلاَثَ عَشْرَةَ . قَالَ أَبُو دَاوُدَ زَادَ أَحْمَدُ بْنُ صَالِحٍ : وَلَمْ يَكُنْ يُوتِرُ بِرَكْعَتَيْنِ قَبْلَ الْفَجْرِ . قُلْتُ : مَا يُوتِرُ قَالَتْ : لَمْ يَكُنْ يَدَعُ ذَلِكَ . وَلَمْ يَذْكُرْ أَحْمَدُ : وَسِتٍّ وَثَلاَثٍ .

Ahmad Ibn Salih kua amesema Muhammad Ibn Salama Al Muradiyu, kua amesema Ibn Wahbi kua amesema Muawwiyah Ibn Salih kua amesema Abd Allah Ibn Qays kua alimuuliza Aisha *Radhi Allahu Anha*: **'Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisa akisali Witr Rakaa ngapi?'**

Ambapo Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Witr kwa Rakaa Nne kisha na Tatu, na Sita kisha na Tatu, na Nane kisha na Tatu, na Kumi kisha na Tatu na alikua hasali chini ya Rakaa Saba.**

Ambapo Ahmad anaendelea kusema kua: 'Alikua hasali Salat Witr yenye Rakaa mbili kabla ya Al Fajr, nami nikamuuliza: 'Alikua akiisali pamoja na nini' ambapo nae akajibu: 'Kamwe hakuwahi kuiwacha' na kwa upande wa Ahmad basi haikutaja maneno sita na tatu'*(Imam Abu Daud)*

Na Imam Ahmad Ibn Hanbal anasema katika Musnad Imam Ahmad kua: '**Qays alimuuliza Aisha *Radhi Allahu Anha* kuhusiana na Sala Salat Al Witr alikua akisali Rakaa ngapi?**'

Na Anasema Imam At Tahawi kua: '**Uqbah Ibn Muslim amesema kua: Nilimuukiza mimi Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anh*u kuhusiana na Salat Al Witr ambapo nae akasema:** '**Jee unaijua Witr ya Mchana?**'

Nami nikajibu: 'Naam, ni Salat Al Maghrib.'

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Naam Umesema kweli.'

Naam..hivyo ni baadhi ya Vithibitisho vya Salat Witr kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa. Ambapo kwa Upande wa wale wanaosali Salat Witr kwa Rakaa mbili kisha kumalizia Moja ambapo Miongoni mwao ni Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hua ni wenye kuegemea kwenye utihibitisho wa Hadith isemayo: '**Sala ya Qiyam Al Layl hua ni Sala ya Rakaa mbilimbili**. **Na hivyo mmoja wetu atakapokhofia kua Asububi inakaribia kuingia basi na amalizie kwa kusali Rakaa moja na hivyo kua ni mwenye Kusali Idadi ya Witr***'(Sahih Imam Bukhari)*

Na anasema Mujaddid Ad Din Imam Abu Fadhl Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Ili kupatanisha Hadith hizi za aina mbili basi tunaona kua imekatazwa kusali Salat Al Witr kwa Rakaa Tatu zenye Tahiyyat mbili ndani yake kama ilivyokua katika Salat Al Maghrib.Na hivi ndivyo ambavyo walivyokua wakisali Waja wema wa vjzazi vya Mwanzo vilivyotangulia kabla.**'

Kwani ingawa imenukuliwa kutoka kwa Muhammad Ibn Nasir kupitka kwa Hasan Al Basr kua Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alikua akinyanyuka kwa ajili ya Rakaa ya Tatu ya Witr kwa Takbirat.

Na Pia imenukuliwa na Miswar Ibn Mahramah kua Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alisali Witr kwa Rakaa 3 na Salam moja mwishoni mwa Rakaa ya tatu.Na pia imenukuliwa na Tawus kutoka kwa baba yake kua Umar Ibn Al Khattab*Radhi Allahu Anhu* alikua akisali Salat Witr kwa Rakaa 3 bila ya kukaa kitako baina ya Rakaa ya pili na ya Tatu.'

Na pia imenukuliwa na Qays Ibn Sad kutoka kwa Ataa na Hammad Ibn Zayd kutoka kwa Ayyub kua Muhammad Ibn Ibn Nasr amesema kua Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*, Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* na Abu Aaliyah kua Walikua wakisali Salat Al Witr kama Salat Al Maghrib. Kama kwamba kukatazwa kwake huko hakujawafikia wao.'

'Hivyo inatakiwa kuifanyia kazi Kauli ya Al Qasim Ibn Muhammad kuhusiana na Kukubalika kwa Kusali Salat Al Wtri kama Rakaa 3, lakini Kutofautiana kwake katika Ulazima wa Kuzisali kama Rakaa 3 basi haujathibitishwa na Hadith sahih.'

Ambapo tunapoiangalia kauli hii ya Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi tunaona kua kulingana na vithibitisho vya Hadith basi ndani yake kuna Aina Tatu za Kusali Salat Al Witr ambazo ni:

1-Kusali Rakaa 3 kama inavyosaliwa Salat Al Maghrib kwa kukaa Tahiyyat 2 ndani yake.

2-Kusali Rakaa 3 kama Salat Al Maghrib lakini ndani yake hua mna Tahiyyat moja tu yaani Kutokaa Tahiyyat ya 1.

3-Kusali Salat Witr Rakaa 3 kwa Kusali Rakaa 2 na kisha kukaa Tahiyyat na Kutoa Salam na kisha kumalizia Rakaa 1 na kisha kukaa Tahiyyat na kutoa Salam.

Na anasema Imam Ibn Hajr wa pili ambae ni Al Faqih Al Muhaqqiq Shaykh ul Islami Imam Shihab Ad Din Abu Fadhl Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii ambae anasema kua: '**Mtu anaposali Sala ya Witr anatakiwa awe na nia ya Kusali Witr, kwa kusali Rakaa mbili kabla ya Kusali Witr Rakaa moja Hivyo mtu anatakiwa azitofautishe Rakaa mbili hizo na moja ya Witr kwa Salam baina yake, kisha asimame na kusali Rakaa moja, ambapo hua ni Sunnah kusoma ndani ya Rakaa 2 kwa Rakaa ya kwanza Surat Al Aala baada ya Surat Al Fatiha na kwa Rakaa ya pili Surat Al Kafirun baada Surat Al Fatiha.'**

Na kisha anaposali Rakaa moja ya Witri asome Sura za Miwshoni mwa Quran baada ya Surat Al Fatiha. Na kutoa Salam baina ya Rakaa za Witr ni Sunnah iliyothibitishwa. Lakini kama Mtu akiunganisha Rakaa 3 kwa pamoja basi hua ni bora kusoma Tahiyyat moja tu katika Rakaa ya Mwisho.'*(Tuhfah Al Muhtaj - Ibn Hajar Al Haytami)*

Na hivyo kulingana na vithibitisho basi Salat Al Witr ziko za aina zifuatazo:

Salat Witr ya Rakaa 3 ambayo husaliwa kama inavyosaliwa Salat Al Maghrib ambapo ndani yake mna Tahiyyat 2 ambao ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Na hii ni kulingana na hadith ya Ummu Ul Muuminin Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua *:Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam:*Alikua akisali Salat Witr Rakaa Tatu na kutoa Salam katika Rakaa ya 3*(Sahih Muslim)*

Salat Al Witr ya Rakaa 3 ambayo hua na Tahiyyat Moja ya Mwisho tu. Hii ni Witr ambayo inakubalika kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal

Na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* iliyoelezewa katika Sunan An Nasai na Mustadrak Al Hakim

Salat Al Witr ya Rakaa 3 ambazo mbili hua zinajitegemea kwa kua na Salam yake kisha bila kupoteza mda Mtu ananyanyuka na kumakizia Rakaa Moja na kutoa Salam

Ambapo huu ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik, na Madhhab ya Imam Al Shafii na hii ni kulingana na Hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu:*

'Kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Salat Al Witr kwa kutenganisha Rakaa mbili, na kutoa Salam na kisha kufuatia Rakaa moja na kutoa Salam*'(Musnad Imam Ahmad)*

Na pia kuna Salat Al Witr ambayo Mtu unaruhusika Kusali Rakaa 5, 7,9 n.k, ambapo huu pia ni Mtizamo wa Wanzuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Na kuna Witr ya Rakaa Moja tu, ambayo inakubalika bila ya tatizo lolote na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Na hii ni kutokana na Hadith isemayo kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam k*ua

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ يَحْيَى، قَالَ حَدَّثَنَا يَعْقُوبُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، قَالَ حَدَّثَنَا ابْنُ أَخِي ابْنِ شِهَابٍ، عَنْ عَمِّهِ، قَالَ أَخْبَرَنِي حُمَيْدُ بْنُ عَبْدِ الرَّحْمَنِ، أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ عُمَرَ، أَخْبَرَهُ أَنَّ رَجُلاً سَأَلَ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَنْ صَلاَةِ اللَّيْلِ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " صَلاَةُ اللَّيْلِ مَثْنَى مَثْنَى فَإِذَا خَشِيتَ الصُّبْحَ فَأَوْتِرْ بِوَاحِدَةٍ

Amesema Muhammad Ibn Yahya kua amesema Yaqub Ibn Ibrahim kua amesema Ibn Aji Shihhab kua amesema Ami yake kua, amesema Humayd Ibn Abd Rahman kua amesema Abd Allah Ibn Umar kua Kuna Mtu alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Sala ya Qiyam Al Laylm ambapo *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* akasema: 'Salat Qiyam Al Layl husaliwa kwa Rakaa mbili mbili na kama mkikhofia Kuingia Alfajir basi malizieni kwa Rakaa Moja.'*(Bukhari na Muslim)***

Ambapo Mtizamo huu wa Rakaa Moja tu peke yake katika Salat Al Witr ni Mtizamo ambao Haupendekezwi kulingana na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhhab ya Imam Malik, na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wanasema kua haipendekezwi kusali rakaa moja ya Witri peke yake, isipokua kama itatokea Mtu anasali nyuma ya Imam anaesali katika mfumo huo basi hua inapendekezwa.

Ambapo amesema Imam Ibn Majah kua:

حَدَّثَنَا عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ إِبْرَاهِيمَ الدِّمَشْقِيُّ، حَدَّثَنَا الْفِرْيَابِيُّ، عَنِ الأَوْزَاعِيِّ، عَنِ الزُّهْرِيِّ، عَنْ عَطَاءِ بْنِ يَزِيدَ اللَّيْثِيِّ، عَنْ أَبِي أَيُّوبَ الأَنْصَارِيِّ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ قَالَ " الْوِتْرُ حَقٌّ. فَمَنْ شَاءَ فَلْيُوتِرْ بِخَمْسٍ. وَمَنْ شَاءَ فَلْيُوتِرْ بِثَلاَثٍ. وَمَنْ شَاءَ فَلْيُوتِرْ بِوَاحِدَةٍ "

Amesema Abd Rahman Ibn Ibrahim AdDimashq kua amesema Al Firyabiyyu kua amesema Az Zuhri kua amesema Ataa Ibn Yazid Al Layth kua Abu Ayub Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Witr ni Haki, hivyo wacha anaetaka Kusali Witr Rakaa 5 na Asali, anaetaka kusali Witr Rakaa 3 na Asali na anetaka Kusali Witr Rakaa 1 na Sali Rakaa moja.'*(Imam Ibn Majah)***

Na amesema Imam Al Bukhari kua:

حَدَّثَنَا الْحَسَنُ بْنُ بِشْرٍ، حَدَّثَنَا الْمُعَافَى، عَنْ عُثْمَانَ بْنِ الأَسْوَدِ، عَنِ ابْنِ أَبِي مُلَيْكَةَ، قَالَ أَوْتَرَ مُعَاوِيَةُ بَعْدَ الْعِشَاءِ بِرَكْعَةٍ وَعِنْدَهُ مَوْلًى لِابْنِ عَبَّاسٍ، فَأَتَى ابْنَ عَبَّاسٍ فَقَالَ دَعْهُ، فَإِنَّهُ صَحِبَ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم.

Amesema Hasan Ibn Bishr kua amesema AlMuafa kua amesema Uthman Ibn Al Aswad kua amesema Imam Ibn Abu Mulaika kua: 'Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* alisali Witr Rakaa moja, baada ya Salat Al Isha. Ambapo Mtumwa alieachwa huru na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alikuwepo mbele yake.

Hivyo Mtumwa huyo akaenda kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na Kumwambia kua amemuona Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* akiwa amesali Salat Al Witr ya Rakaa moja.

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: Mwachie kwani yeye alikua ni Miongoni mwa Masahaba waliokua na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*'*(Sahih Bukhari)***

Na Imam Malikamesema katika kitabu chake cha Muwwata kua:

وَحَدَّثَنِي عَنْ مَالِكٍ، عَنْ نَافِعٍ، أَنَّهُ قَالَ كُنْتُ مَعَ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ بِمَكَّةَ وَالسَّمَاءُ مُغِيمَةٌ فَخَشِيَ عَبْدُ اللَّهِ الصُّبْحَ فَأَوْتَرَ بِوَاحِدَةٍ ثُمَّ انْكَشَفَ الْغَيْمُ فَرَأَى أَنَّ عَلَيْهِ لَيْلاً فَشَفَعَ بِوَاحِدَةٍ ثُمَّ صَلَّى بَعْدَ ذَلِكَ رَكْعَتَيْنِ رَكْعَتَيْنِ فَلَمَّا خَشِيَ الصُّبْحَ أَوْتَرَ بِوَاحِدَةٍ .

Amesema Yahya kua amesema Malik Kua amesema Nafii kua amesema kua Mimi nilikua na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*katika Mji wa Makkah, Anga ilikua imejaa Mawingu na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akikhofia kua Alfajir inakaribia kuingia hivyo akasali Rakaa moja ya Witr, na kisha mara mawingu yakaondoka na akaona kua bado ni usiku, hivyo akasali Sala yake rakaa mbili na kisha akongezea moja, na kisha akaongezea Rakaa mbili mbili hadi alipokhofia kuingia kwa Alfajir akasali Rakaa moja ya Witr.'*(Muwwata Imam Malik)*

Na Imam An Nasai ana Hadith isemayo kua:

أَخْبَرَنَا الْحَسَنُ بْنُ مُحَمَّدٍ، عَنْ عَفَّانَ، قَالَ حَدَّثَنَا هَمَّامٌ، قَالَ حَدَّثَنَا قَتَادَةُ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ شَقِيقٍ، عَنِ ابْنِ عُمَرَ، أَنَّ رَجُلاً، مِنْ أَهْلِ الْبَادِيَةِ سَأَلَ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَنْ صَلاَةِ اللَّيْلِ قَالَ " مَثْنَى مَثْنَى وَالْوَتْرُ رَكْعَةٌ مِنْ آخِرِ اللَّيْلِ

Amesema Al Hasan Ibn Muhammad kua amesema Affan kua amesema Hammam kua amesema Qatadah kua amesema Abd Allah Ibn Shaqiq kua Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* Mmoja miongoni mwa Mabedui alimuuza *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*kuhusiana na Sala za Usiku ambapo nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Rakaa Mbili mbili na Rakaa Moja ya Witr mwishoni mwa Usiku.'*(Sunnan An Nasai)***

Na akasema tena Imam An Nasai kua:

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ سَلَمَةَ، قَالَ أَنْبَأَنَا ابْنُ الْقَاسِمِ، عَنْ مَالِكٍ، قَالَ حَدَّثَنِي مَخْرَمَةُ بْنُ سُلَيْمَانَ، عَنْ كُرَيْبٍ، أَنَّ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ عَبَّاسٍ، أَخْبَرَهُ أَنَّهُ، بَاتَ عِنْدَ مَيْمُونَةَ أُمِّ الْمُؤْمِنِينَ - وَهِيَ خَالَتُهُ - فَاضْطَجَعَ فِي عَرْضِ الْوِسَادَةِ وَاضْطَجَعَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم وَأَهْلُهُ فِي طُولِهَا فَنَامَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم حَتَّى إِذَا انْتَصَفَ اللَّيْلُ أَوْ قَبْلَهُ قَلِيلاً أَوْ بَعْدَهُ قَلِيلاً اسْتَيْقَظَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَجَلَسَ يَمْسَحُ النَّوْمَ عَنْ وَجْهِهِ بِيَدِهِ ثُمَّ قَرَأَ الْعَشْرَ الآيَاتِ الْخَوَاتِيمَ مِنْ سُورَةِ آلِ عِمْرَانَ ثُمَّ قَامَ إِلَى شَنٍّ مُعَلَّقَةٍ فَتَوَضَّأَ مِنْهَا فَأَحْسَنَ وُضُوءَهُ ثُمَّ قَامَ يُصَلِّي قَالَ عَبْدُ اللَّهِ بْنُ عَبَّاسٍ فَقُمْتُ فَصَنَعْتُ مِثْلَ مَا صَنَعَ ثُمَّ ذَهَبْتُ فَقُمْتُ إِلَى جَنْبِهِ فَوَضَعَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَدَهُ الْيُمْنَى عَلَى رَأْسِي وَأَخَذَ بِأُذُنِي

الْيُمْنَى يَفْتِلُهَا فَصَلَّى رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ رَكْعَتَيْنِ ثُمَّ أَوْتَرَ ثُمَّ اضْطَجَعَ حَتَّى جَاءَهُ الْمُؤَذِّنُ فَصَلَّى رَكْعَتَيْنِ خَفِيفَتَيْنِ

Amesema Qurayb *Radhi Allahu Anhu* kuaamesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allah Anhu*ambae alikua amelala kwa Maimuna Mke wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*Ambae ni Mama yake mdogo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*kua: 'Nililala mimi pembeni ya *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* na mke wake. *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*alilala hadi Usiku wa manane au kabla yake kidogo au baada yake kidogo, na kisha *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*akaamka na kuufuta Usingizi kutoka katika macho yakekwa mikono wake na kisha akasoma Aya kumi za mwishoni mwa Surat Al Imran, na kisha akanyanyuka na kuelekea kwenye kibuyu chake cha Maji, ambacho kilikua kimetundikwa na kisha akatia Udhu na kisha *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*akasimama na kusali.'

Abd Allah In Abbas *Radhi Allahu Anhu* anasema kua: 'Na mimi nikasimama nakufanya kama alivyofanya yeye na niakenda kusimama pembeni yake *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam. Na Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*akaukamata mkono wangu na kuuvuta na kisha akasalia Raka mbili, kisha akasali Rakaa mbili kisha akasali Rakaa mbili,kisha akasali Rakaa mbili kisha akasali Rakaa mbili na kisha akasali Rakaa mbili na kisha akasali Rakaa Moja Witr na kisha akalala hadi alipoadhini Muadhini na kisha akasali Rakaa mbili zilizozokua fupi.''*(Sunan An Nasai)***

Na pia Imam Al Bukhari ana hadithi sahih zisemazo kua Saad Ibn Abi Waqas *Radhi Allahu Anhu*, Muawwiyah Ibn Abi Sufyan *Radhi Allahu Anhu*, walikua wakisali Salat Witr ya Rakaa moja, na Imam Al Bayhaqi pia katika Sunan Al Kubra ana Hadith sahih isemayo kua Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* alisali Salat Al Witr ya Rakaa moja.

Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani amesema kua: '**Imethibitishwa na Hadith nyingi kua Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua walikisali Rakaa moja ya Witr bila ya Kusali Rakaa mbili kabla yake. Na imenukuliwa na Muhamamd Ibn Nasr na wengineo kupitia katika Sahih Hadith yenye Sanad Sahihkutoka kwa Saib Ibn Yazid kua Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* alikua akisoma Qur'an usiku mmoja ndani ya Sala ya Rakaa moja bila ya kuogeza Rakaa nyengine yeyote ndani yake.**'

'Na pia ndani ya Maghazi tunanukuu Hadith ya Abd Allah Ibn Thalabah *Radhi Allau Anhu* kua SaadIbn Abi Waqas *Radhi Allahu Anhu* alikua akisali Witr Rakaa moja na katika Manaqib kuna Hadith isemayo kua Muawwiyah *Radhi Allahu Anhu* alikua akisali Witr Rakaa moja ambayo imekubaliwa na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu.*'*(Fat-h Al Baari)***

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Yahya Sharaf An Nawawi kua:'**Katika Madhhab yetu ya Imam Al Shafii basi hua haipendekezwi kusomwa kwa Qunut katika Witr ya mwezi wa Ramadhan zaidi ya Ndani ya Nusu ya pili ya Mwezi wa Ramadhani'***(Rawdha Talibin)*

Na akasema Shaykh Ul Islami Imam Ibn Abd Al Barr Al Maliki Al Andalus kua:**'Ama kuhusiana na Imam Al Shafii alipokua katika Ardhi ya Iraq basi Mtizamo wake ulikua kama alivyonukuu Imam Al Zafarani kua alikua akisoma Qunut katika Salat Al Witr kuanzia katika Nusu ya Pili ya mwezi wa Ramadhani. Kwani Imam Al Shafii Alikua hasomi Qunut katika Salat Al Witr ndani ya mwaka Mzima isipokua ndani ya Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhani. Na Imam Al Shafii**

alipokua Nchini Misri alitoa Fatwa kua Mtu hutakiwa Kusoma Qunut katika Salat Al Fajr ya kila Siku na pale anapotaka Kusoma Qunut kwa Ajili ya kuwaombea Watu basi asome katika Sala nyengiezo.' Ambapo Mimi (Imam Ibn Abd Al Barr) sijaona Kasoro yeyote katika Fatwa zake hizi.'*(Al Istidhkar)*

Ambapo amesema Imam Al Zafarani Al Shafii kua: '**Imam Al Shafii amependekeza Mtizamo wa kua Qunut katika Salat Al Witr isomwe ndani ya Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhani tu, na isisomwe mwaka mzima**.'*(Tuhfah Al Ahwadhi)*

Na anasema Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Maliki Al Qurtubi kua: '**Riwaya zinaozungumzia kuhusiana na Kusomwa kwa Qunut katika Nusu ya Pili ya mwezi wa Ramadhani zimenukuliaa kutoka kwa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Ubay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu*Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Imam Muhammad Ibn Sirin, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Az Zuhri, Imam Yahya Ibn Wathaab, Imam Malik, Imam Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Ibn Al Mundhir n.k.'**

Na Imam Ibn Jurayj alimuuliza Imam Ataa kua kusema: 'Hivi Jee kuna Qunut katika Mwezi wa Ramadhan?'

Na Imam Ataa akasema 'Mtu wa mwanzo kuanza kusoma Qunut katika Mwezi wa Ramadhan alikua ni Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.'*

Imam Ibn Jurayj akauliza: 'Katika Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhani au'?

Imam Ataa akajibu kwa kusema: 'Naam!'*(Al Istidraak)*

Na ingawa kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii Qunut hii ya Salat Al Witri ya Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan hua ni Wajib kama tulivyoona na hivyo kua ni Sunna Ab'aadh ambayo kama hukuitekeleza basi hukubidi kuleta Sijdat Sahw.

Ambapo Mtizamo wa kua Qunut inatakiwa kusomwa ndani ya mwezi mzima wa Ramadhan katika Sala ya Witr hua ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik. Na kwa upande wa Madhhab mengine Qunut hii hua ni Sunnah inayopendekezwa.Na hivyo kumaanisha kua anaetaka anaweza kuisoma na atalipwa na asietaka anaweza akaachana nayo na Sala yake haitokua na kasoro na wala hatopata Dhambi.

Hivyo tunaporudi kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunakumbushana kua kwa wale ambao hawakuihifadhi Qunut au hawaijui na hivyo hawajui wasome nini basi Wanazuoni wanasema kua unaweza Kusoma Dua yeyote uijuayo, ila huani vizuri ndani yake Dua hio iwe kuna kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na pia Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na kwa upande mwengine basi tunakumbushana pia kua Ingawa amesema Imam Ibn Abd Al Barr kua amesema Imam Ataa amesema kua alieanzisha Qunut Katika Witr ya Nusu ya pili ya Mwezi wa Ramadhani.Lakini hata hivyo tusisahau kua miongoni mwa Hadith za Qunut basi ziko kadhaa zinazothibitisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisoma Qunut katika Salat Al Witr ikiwemo hadith ya Hasan Ibn Ali Ibn Ali Talib *Radhi Allahu Anhu* ambayo inayoonesha namna *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyokua akiaafundisha Wajuu zake hao kusoma Qunut kwenye Sala ya Witr.

Kwani amesema Imam Al Bayhaqi kua amesema Imam Abbas Ibn Al Walid Ibn Mazid kua amesema Baba yake kua:**'Mimi nilimuuliza Al Awzai kuhusiana na Qunut katika mwezi wa Ramadhani.'**

Ambapo Imam Al Awzai akasema: '**Ama kuhusiana na Jamaa ya Msikitini ambayo ndani yakehua wanasoma Qunut tangu mwanzo wa Mwezi wa Ramadhan hadi mwisho, basi Watu wa Madina husoma Qunut kuanzia katika Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan.Na ingawa kuna hadith inayonasibishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya hilo, lakini hadith hio haina nguvu.'***(Sunan Al Kubra Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo anasema Imam Muhammad Abd Allah Al Azraqi katika kitabu chake cha *Akhbar Makkah wa Ma Jaa Fii min Al Akhbar* basi tunaona anasema kua: '**Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* amesema kua aliwakuta watu wa Makkah wakiwa hawasomi Qunut katika Salat Al Witr isipokua katika Nusu ya pili ya Mwezi wa Ramadhani.'**

Ambapo anasema Imam Al Baji Al Maliki katika *Sharh Al Muwwata* kua:**'Amesema Imam Malik kua amesema Araj kua: Mimi sikuwahi kukutana na Watu katika mwezi wa Ramadhan isipokua walikua wakiwalaani Makafiri.'**

Imam Al Baji anaendelea kusema kua: **'Watu waliokusudiwa na riwaya hii ni Masahaba *Radhi Allahu Anhum.*Na kuwalaani kwao Makafiri ni kupitia katika Visomo vyao vya Qunut katika Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhani katika Salat Al Witr.Na hakuna kutokukubaliana kwa Wanazuoni juu ya kua Qunut hua inakusudiwa hususan katika Nusu ya Pili ya mwezi wa Ramadhan katika Witr.'***(Al Muntaqa Sharh Al Muwwata)*

Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Jalal Ad din Al Suyuti pia ameunga mkono maneno ya Imam Al Baki katika kitabu chake cha Tanwir Al Hawalik kua: '**Hakuna kutokukubaliana kuhusiana na Qunut katika Salat Al Witr ya Ramadhan hua ni katika Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan.'**

Ama kwa upande wa Imam Ibn Khuzaymah nae amenukuu pia Hadith hii ya Araj aliyoinukuu Imam Malik katika Muwwata.Lakini yeye kwa upande wake ameweka wazi hasa kua Kulaaniwa huko kwa Makafiri ilikua ni katika Qunut ya Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan.

Na kwa upande mwengine basi Imam Al Bayhaqi tena pia ana Hadith isemayo kua: '**Amesema Abu Abd Allah Al Hafidh kua amesema Abu Bakr Ibn Hasan Al Qadhi kua amesema Abu Al Abbas Muhammad Ibn Yaqub kua amesema Abbas Al Duri kua: 'Amesema Hasan Ibn Bishr kua amesema Al Hakam Ibn Abd Al Malak kua amesema Qatadah kua amesema Hasan kua:** '**Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alikua akitusalisha sisi katika kipindi cha Utawala wa Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* kwa mda wa Siku 20 na kisha akaacha baadhi wakaasema kua Ameingia kwenye Riadha:** '**Baada ya hapo Abu Halima Muadh Al Qari akawa anatusalisha na alikua akisoma Qunut***'(Sunan Al Kubra)*

Na akasema tena Imam Al Bayhaqi kua: '**Amesema Abu Hazim Al Hafidh kua amesema Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhammad Ibn Al Husayn Al Masarjisi kua amesema Shaybah Ibn Faruq Al Ubulli kua amesema Salma Ibn Miskin kua:Muhammad Ibn Sirin alikua hapendi kusoma Qunut isipokua katika Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan.'**

Na akasema Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kua: '**Qunut hua ni katika Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan.'***(Sunnan Al Kubra)*

Ama tunapoendelea kuangalia kuhusiana na Qunut Katika Salat Al Witr basi tunaona kua anasema Imam Taj Ad Din Al Subki katika Tabaqaat Shafiyat Al Kubra kua: '**Hakika mimi nimekutana na Ufupisho wa Kitabu cha Abu Al Fadhl Ibn Abdan kitwacho Sharh Al Ibadat ambacho Kitabu chake cha**

asili hasa nimekikuta katikaHazina ya Waqf ya Ibn Urwa katika Masjid Umayyad mjini Dimashq, ambapo amesema Ibn Abdan kua:Ama kuhusiana na Mtizamo wangu mimi juu ya Qunut katika Salat Al Witri basi ni kua Inasomwa Mwaka mzim*a.'* *(Tabaqat Al Shafiyya Al Kubra)*

Ambapo huu pia ni mmoja kati ya Mtizamo wa baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Akiwemo Imam Abu Fadhl Ibn Abdan Al Shafii, Imam Abu Abd Allah Al Zubayr Al Shafii, Imam Abu Walid Al Nishapuri na Imam Abu Mansur Al Mihran.

Na kutokana na Mtizamo huo basi tunaona kua Imam Al Ruyani Al Shafii amesema kua : '**Qunut ndani ya Salat Witr kwa mwaka mzima hua haina tatizo na wala haikirihishi**. **Na hii haimpekei Mtu kuleta Sijda Sahw kama hakuisoma pale inapokua si ndani ya Nusu ya pili ya mwezi wa RamadhanNa huu ndio mtizamo wa Wanazuoni wa Tabarstan'**(*Rawdah Al Talibin)*

Ambapo Mtizamo huu pia unaungwa mkono na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi, kwa kusema kua : '**Kwa Ikhtiyar (mtizamo wangu mimi mwenyewe na wala si Mtizamo wa Madhhab) basi Mtizamo huu pia una nguvu na hii ni kulingana na Uthibitisho wa Hadith ya Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu'***(*Sharh Al Muhadhdhab)*

Na pia Imam An Nawawi amesema tena katika Al Tahqiq kua: '**Kusoma Qunut katika Salat Al Witr ya ndani ya Mwaka mzima ni Mtizamo wa Al Mukhtar.' (Ninaoupendelea)**

Na ingawa Imam Taj Ad Din Al Subki amesema hivyo kuhusiana na Qunut katika Mwaka mzima lakini kwa upande wa Baba yake Imam Taj Ad Din Al Subki Al Shafii ambae ni Imam Taqi Ad Din Al Subki Al Shafii basi amesema kama alivyosema mwanawe kua: '**Lakini hata hivyo Baba (Imam Taqi Ad Din Al Subki) amefanya Tawaqquf (Amejizuia kutoa Fatwa juu ya Jambo hilo) kuhusiana na Mtizamo wa Kujitegemea wa Imam An Nawawi (wa kua Imam An Nawawi anapendelea Qunut ndani ya Witri ya mwaka mzima) kwani amesema kua:Hakuna Uthibitisho uliokua wazi wa Hadith unaothibitisha hivyo**'*(Tabaqat Al Shaffiyah Al Kubra)*

Naam..hivyo tuhitimishe kuhusiana na Wajibu wa Qunut ya Salat Al Witr kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kama anavyosema Al Muhaqqiq Al Faqih, Imam Abu Fadhl Shihab Ad Din Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: '**Mtizamo unaotegemewa na kukubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Qunut katika Salat Al Witr basi ni kua hua haipendekezwi Isipokua katika Salat Al Witr ya Nusu ya pili ya Mwezi wa Ramadhani tu.'***(Tuhfah Al Muhtaj)*

QUNUT NAZILA

❖❖❖

Neno Nazil ni lenye kutokana na neno Nazala ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kushusha, Kuteremsha, Kuja chini, Kuweka Chini

Neno Nazala ndio lililotoa neno Nuzulun ambalo humaanisha Vitu vya Tunu anavyotayarishiwa Mgeni.

Na pia likatoa neno Manzil ambalo humaanisha Makazi, Kituo au Jengo.

Na neno Nazala ndio lililotoa neno Nazil ambalo humaanisha Mshuko wa Jambo au Mtokeo wa Tukio.

Hivyo Qunut Nazila imeitwa Hivyo kwa sababu hua ni Dua ya Qunut inayosomwa pale inapotokea Jambo au Tukio ambalo linaleta Athari mbaya au Madhara kwa Mtu, kwa Jamii au kwa Ummah wa Kiislam kwa Ujumla.

Hivyo Qunut Nazila hua inaweza kusomwa na Mtu mmoja, iwe Msikitini au Nyumbani kwake, iwe Mwanamme au Mwanammke kulingana na yaliyotokea, au inaweza kusoma kwa Jamaa Msikitini, Uwanjani au Misikitini.

Na hua inapendekezwa kua pale Mtu au Jamii inapokutwa na Janga iwe la Maradhi, Uadui, Udhalimu n.k kusoma Qunut Nazila hadi Janga au Tatizo hilo litakapoondoka au litakapoisha kulingana na madhara yake.

Kwani Qunut Nazila ni miongoni mwa Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pale baada ya Vita vya Uhud ambavyo ni vita vya pili katika historia ya Uislam.

Ambapo katika vita hivyo Waislam walishindwa na matokeo yake Makafiri wa Makkah waliwaua Waislam wengi sana na pia Makafiri hao wakawavamia Waislam 80 katika maeneo ya Al Raji na Bir Maun.

Waislam hao 80 walikua ni Masahaba Wanazuoni *Radhi Allahu Anhum* waiohifadhi Qur'an ambao walitumwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kuwafundisha Quran na Dini ya Kiislam baadhi ya Watu wa Vijiji vya mbali na Mji wa Madina katika Maeneo ya Najd.

Na mwanzo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwatuma Masahaba 10 ambao walipofika katika maeneo ya Al Raji wakavamiwa na watu wa Kabila la Adal na Al Qarra ambao wakawaua Masahaba Wanane kati ya Kumi na kisha Wawili waliobakia wakawakabidhi kwa Maquraysh ambao wakawaua Waislam hao.

Na kabla ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kupata habari za Mauaji hayo basi aliwatuma Masahaba Wanazuoni 70 *Radhi Allahu Anhu* kuelekea katika upande mwengine kwa ajili ya kuwafundisha Qur'an watu wa Malik Ibn Amir. Wanaoishi katika Maeneo ya Najd ambao waliomba wapelekewe Waislam watakaowafundisha Dini ya Uislam.

Na ingawa mwanzoni *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisita kutuma Masahaba zake hao kwa sababu ya Ukatili na Uadui wa Watu wa Najd dhidi ya Uislam.Lakini hata hivyo mwishoni alikubali baada ya kuahidiwa Usalama wa Masahaba zake hao na Malik Ibn Amir.

Na baada ya Masahaba hao kuondoka katika Mji wa Madina basi njiani wakavamiwa na Watu wa Najd waliokua wakiongozwa na Amr Ibn Tufayl na wakauliwa wote isipokua Mmoja tu ambae alijaaliwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kukimbia na kuwasili katika Mji wa Madina huku akiwa taaban kutokana na Majeraha aliyokua nayo.

Kama anvyosema Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* katika hadith ifuatayo:

أَنَّ رِعْلاً، وَذَكْوَانَ وَعُصَيَّةَ وَبَنِي لَحْيَانَ اسْتَمَدُّوا رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَلَى عَدُوٍّ، فَأَمَدَّهُمْ بِسَبْعِينَ مِنَ الأَنْصَارِ، كُنَّا نُسَمِّيهِمُ الْقُرَّاءَ فِي زَمَانِهِمْ، كَانُوا يَحْتَطِبُونَ بِالنَّهَارِ وَيُصَلُّونَ بِاللَّيْلِ، حَتَّى كَانُوا بِبِئْرِ مَعُونَةَ قَتَلُوهُمْ، وَغَدَرُوا بِهِمْ، فَبَلَغَ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم، فَقَنَتَ شَهْرًا يَدْعُو فِي الصُّبْحِ عَلَى أَحْيَاءٍ مِنْ أَحْيَاءِ الْعَرَبِ، عَلَى رِعْلٍ وَذَكْوَانَ وَعُصَيَّةَ وَبَنِي لَحْيَانَ.

Watu wa Rila na Dhakwan, Usaiah na Bani Lahyan walimuomba *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* awapatie Vijana amba watawaunga mkono dhidi ya maadui zao. Na hivyo akawapatiavijana 70 kutoka katika Watu wa Ansar ambao sisi tlkua tukiwaita kama Al Qura katika maisha yao. Kwani walikua ni wenye kukusanya Kuni katika wakati wa mchana na kusali katika wakati wa Usiku. Na walipokua katika Kisima cha Al Mauna basi Makafiri wakawauwa wote kwa kuwasaliti. Na hivyo habari hii ilipomfikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* akasoma Qunut kwa mwezi mzima katika Sala ya Alfajir kuwaombea adhabu baadhi ya Makabila ya watu hao wa Kiarabu na baadhi ya watu wa Rila, Dhakwan Usaiya na Bani Lahyan.*(*Sahih Bukhari*)**

Kwani tukio hili lilikua ni Janga kubwa sana kwa Uislam na lilimhuzunisha sana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Kama anavyosema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:

Hakika mimi kamwe sikuwahi kumuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa na huzuni kubwa sana kama alivyokua na huzuni kutokana mauaji ya Masahaba hao 70 ambao walikua ni wasomaji wa Qur'an ambao waliuliwa katika maeneo ya Al Maauna. Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawasomea Qunut Nazila kwa mda wa Mwezi mzima Makafiri waliowaua Waislam hao.'*(*Sahih Muslim*)**

Na katika hadithi nyengine basi anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم كَانَ إِذَا قَالَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ فِي الرَّكْعَةِ الْآخِرَةِ مِنْ صَلَاةِ الْعِشَاءِ قَنَتَ اللَّهُمَّ أَنْجِ عَيَّاشَ بْنَ أَبِي رَبِيعَةَ اللَّهُمَّ أَنْجِ الْوَلِيدَ بْنَ الْوَلِيدِ اللَّهُمَّ أَنْجِ سَلَمَةَ بْنَ هِشَامٍ اللَّهُمَّ أَنْجِ الْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اللَّهُمَّ اشْدُدْ وَطْأَتَكَ عَلَى مُضَرَ اللَّهُمَّ اجْعَلْهَا عَلَيْهِمْ سِنِينَ كَسِنِي يُوسُفَ

Wakati *Rasul Allah Salallauhu Alayhi wa Salam* alipokua askiema: '*Sami Allahu LimanHamida*' katika Rakaa ya mwisho ya Salat Al Isha basi alikua akimuomba*Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kusema: ' Ya Allah muokoe Aiyash Ibn Abi Rabia, Ya Allah muokoe Al Walid Ibn Walid, Ya Allah waokoe waliokua dhaifu miongoni mwa Waumini, Ya Allah kua mgumu kwa watu wa Kabila la Mudar, Ya Allah wajaalie miaka ya Ukame kama ulivyojaalia katika miaka ya Nabii Yusuf.'

Hivyo ili tuweze kutofautisha basi na tuangalie mifano ya Kisomo cha Qunut Nazila ambayo hua ni kama ilivyoelezewa na Imam Al Tirimdhii ambavyo ni ifuatavyo:

اللَّهُمَّ اهْدِنِي فِيمَنْ هَدَيْتَ، وَعَافِنِي فِيمَنْ عَافَيْتَ، وَتَوَلَّنِي فِيمَنْ تَوَلَّيْتَ، وَبَارِكْ لِي فِيمَا أَعْطَيْتَ، وَقِنِي شَرَّ مَا قَضَيْتَ، فَإِنَّكَ تَقْضِي وَلاَ يُقْضَى عَلَيْكَ، وَإِنَّهُ لاَ يَذِلُّ مَنْ وَالَيْتَ، تَبَارَكْتَ رَبَّنَا وَتَعَالَيْتَ اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَالْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ، وَأَلِّفْ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ، وَأَصْلِحْ ذَاتَ بَيْنِهِمْ، وَانْصُرْهُمْ عَلَى عَدُوِّك وَعَدُوِّهِمْ. اللَّهُمَّ الْعَنْ كَفَرَةَ الْكِتَابِ الَّذِينَ يُكَذِّبُونَ رُسُلَك وَيُقَاتِلُونَ أَوْلِيَاءَك. اللَّهُمَّ خَالِفْ بَيْنَ كَلِمَتِهِمْ، وَزَلْزِلْ أَقْدَامَهُمْ، وَأَنْزِلْ عَلَيْهِمْ بَأْسَك الَّذِي لَا يُرَدُّ عَنْ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ

***Allahuma Ihdini Fii Man Hadayt* - Ya Allah Niongoze Kama Ulivyowaongoza Waliongoka.**
***Waafini Fiiman aAafayt* - Na Niokoe kama Ulivyowaokoa Waliokoka.**
***Watawalani Fiiman Tawalayh* - Na Nisimamie kua miongoni mwa Uliowasimamia.**
***Wabarik Fiiman A'atayt* - Na Nibariki Katika Ulichonipa.**
***Waqinni Sharran Ma Qadhait* - Na Nikinge na Shari Ulizoniadikia zinifike.**
***Innaka Taqdhi wala Yuqdha Aalayk* - Kwa Hakika wewe ndie Mwenye Kutaka Na Hakuna Anaeweza kutaka Dhidi yako.**
***Wainnahu la Yadhilu Man Walayt* - Na kwa Hakika Hadhaliliki Yule Ulie karibu nae.**
***Wala YaiI'zu Man Adayt* - Na Wala Hatukuki Alie Adui Yako.**
***Tabarakta Rabbana Wa TaA'alayt* - Baraka zote ni Zako Ewe Mola wetu na Utukufu ni wako.**
***Allahuma Ighfirly Al Muuminina wa al Muuminat* - Ya Allah Wasamehe Waumini wa Kiume na Waumini wa Kike**
***Wa Al Muslimina wa Al Muslimat* -Na Waislam wa Kiume na Waislam wa Kike**
***Wa Alif bayna Quluubihim*- Na waunganishe Baina Nyoyo zao**
***Waaslih Dhata Baynihim* - Na Wasuluhishie Baina ya Matatizo yao**
Wansurhum bayna A'ala Aduwik wa Aaduhim - Na Wanusuru Dhidi ya Maadui zako na Maadui zao
***Allahuma alAan Kafarata Al Kitabi* - Ya Allah Walaani Waliokufuru Vitabu vyako**
***Alladhiina Yukadhiibuna Rasulaka* - Wale ambao wamewakadhibisha Mitume wako**
***Wayuqatiluuna Awliyaaik* - Na Wakawaua Mawalii wako**
***Allahuma Khalif Bayna Kallimatihim* - Ya Allah Waparaganyie Makubaliano yao**
***Wazalzilu Aqdamahum* - Na Itetemeshe Miguu yao**
***Wanzala Aalayhim Baasaka* - Na Washushie Adhabu**
Alladhi la yuraddu aan Al Qawmi Mujrimin* - Ambayo haitogeuka dhidi Yao Watu waovu.'(Imam At Tirmidhii)*

Naam..huo ni mmoja kati ya mifano ya Kisomo cha Qunuti Nazila ambayo hua ni kwa Ajili ya Maadui wa Uislam. Ambapo tunapoangalia mifano wa Qunuti Nazila kwa ajili ya Kuondolewa Mitihani kama ya Maradhi, Njaa, Ukame ambayo hua inahusishwa kua ni miongoni mwa Adhabu za A*llah Subhanah Ta'ala* hapa Duniani lakini pale inapokua imezidi na hakuna linalofanyika basi hua inasomwa Qunut ya Kawaida kisha inasomwa Dua ifuatayo:

اللهم إياكَ نعبد، ولك نصلي ونسجد، وإليك نسعى ونحفد، نرجو رحمتك ونخشى عذابك، إن عذابك الجد بالكفار ملحق

***Allahuma Iyyaka Naabudu* - Ya Allah Hakika Sisi Tunakuabudu wewe tu.**

***Walaka Nusalii wanasjud* - Na wewe ndie Tunaosali kwa ajili yake na Tunaekusujudia.**
***Wailayka NasiAui Wanahfid* - Na kwako wewe ndiko tunakoelekeza Juhudi zetu zote Kiibada.**
***Narjuu Rahmatik wanakhshuu Aadhabik* - Turudishie Rehma zako kwani Tunaogopa Adhabu zako.**
Inna Aadhabik AlJadi Bi Al Kufaar Malhu*q -Kwani kwa Hakika Adhabu zako hua zinawastahiki Makafiri.(Sunan Imam Al Bayhaqi)***

Na pia mfano mwengine ambao ni muhimu kwa wakati huu wa Uhai wetu ni Kwa ajili ya Kuwaombea Waislam wa Wapalestina, Lebanon n.k kutokana na Mauaji na Dhulma wanazofanyiwa, hivyo Qunut Nazila yake hua baada ya Qunut ya Kawaida kisha Unasema:

اَللَّهُمَّ انْصُرْ إِخْوَانَنَا الْمُسْتَضْعَفِيْنَ فِي غَزَّةَ وَفِيْ فِلِسْطِيْنَوَفِيْ كُلِّ مَكَانٍ، يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِيْنَ. اَللَّهُمَّ خُذْ بِأَيْدِيْهِمْ، وَاحْفَظْهُمْ، وَالْطُفْ بِهِمْ، وَكُفَّ أَيْدِيَ الْمَاكِرِيْنَ بِهِمْاللَّهُمَّ كُنْ عَوْنًا لَهُمْ مِنْ شُرُوْرِ الظَّالِمِيْن، وَارْفَعْ عَنْهُمُ الْأَذَى وَالظُّلْمَ، وَجَمِيْعَ أَنْوَاعِ الْفِتَنِ وَالْمِحَنِ، مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ، وَالْطُفْ بِهِمْ فِيْ مَا جَرَتْ بِهِ الْمَقَادِيْرُ، فِيْ عَافِيَةٍ وَسَلَامَةٍ، بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِيْنَ

***Allahumma Nsur Ikhwanina Al Mustadhaafina* - Ya Allah Wanusuru Ndugu zetu waliodhoofika Kinguvu na Kiuwezo.**
***Fi Ghazzah, Wa Filistina wa Lubnan* - Katika Ardhi ya Gaza, Na Palestina na Lebanon.**
***Wa fii kulli Makan* - Na Katika Kila Sehemu.**
***Ya Arhama Rahiimin* - Ewe Mwingi wa Rehma na Huruma.**
***Allahuma Khudh Bi Aydihim* - Ya Allah Washike kwa Mikono yao.**
***Wahfidhhum* - Na Wahifadhi.**
***Waltuf Bihim* - Na Kua na huruma Juu yao.**
***Wa kuffa Aydil Makirrina Bihim* - Na Izuie Mikono ya Wanaopanga Njama dhidi yao.**
***Allahuma Kun Auna lahum* - Ya Alla kua Msaidizi kwao.**
***Min Shururi Dhalimin* - Kutokana na Shari za Wanaowadhulumu.**
***Waarfaa Anhum Al Aadha wa Dhulm* - Na Waondolee Udhia na Dhulma.**
***Wajamiia Anwail Fitan* - Na kila aina ya Fitna na Mitihani.**
***Wa Madhahara minha wa ma Batan* -Na Kila kilichomo ndani yake kwa uwazi na kwa uficho.**
***Waltuf bihim fi majaraat bihi Al Maqadir* - Na kua na huruma nao kutokana na kile ulichowakadiria.**
***Fi Afiyatin Wasalamatin* - Kwa Afya na kwa Kiusalama.**
***Birahmatika Ya Arhama Rahimiin* - Kwa Rehma zako ewe Miwngi wa Rehma na Huruma Amiin.**

Mfano mwengine ni Qunut ya Toba ambayo ni kama ifuatavyo:

اللهم إنا نستعينك ونستهديك، ونستغفرك ونتوب إليك، ونؤمن بك ونتوكل عليك، ونثني عليك الخير كله، نشكرك ولا نكفرك، ونخلع ونترك من يفجرك.

Ya Allah tunaomba msaada wako na uongofu wako, tunaomba msamaha wako na tunatubu kikweli juu yako, Tunathibitisha kua Tunakuamini kikweli na tunakutegemea wewe ipasavyo katka kila kitu chetu, tunakutukuza kwa kila lenye kheri kutoka kwako na tunakushukuru na

kujitahidi kutokua na shukurani kutokana na neema zako juu yetu, tunajitenga na kujiweka mbali na wale wenye kukukataa wewe.

Na pia mfano mwengine wa Qunut ya kuomba kujiondoelea matatizo mbali mbali ya kimaisha katika Jamii ni:

اللهم احفظنا، وارحمنا، وانصرنا، وفرج كربنا وكرب المسلمين، اللهم اكفنا والمسلمين شر مصائب الدنيا والدين، أصلحنا وأصلح من في صلاحه صلاح المسلمين، لا تهلكنا، وأهلك من في هلاكه صلاح المسلمين. اللهم اسقنا الرحمة واللطف والعافية والبركة ولا تجعلنا من المحرومين.

Ya Allah tulinde, turehemu, tupe ushindi, tupunguzie dhiki zetu na dhiki za Waislamu wote. Utukinge sisi na Waislamu wote kutokana na shari za misiba katika mambo haya ya kidunia na kidini. Tuongoze kwenye uwongofu, na uwaongoze wale ambao urekebishaji wao unaleta wema kwa Waislamu. Utuepushe na maangamizo, na wakabiliane nayo wale ambao kuondolewa kwao kunaleta manufaa kwa Waislamu. Ewe Allah Subahanah wa Ta'ala, tumiminie rehema, upole, wema, na baraka zako, wala usitunyime neema Zako.

Na pia Dua ifuatayo:

اللهم اصرف عنا وعن المسلمين الأذى والمحن والجور والظلم وكل البلايا والأمراض والفتن والضلال والجهل ما ظهر منها وما بطن. اللهم أنجِ المستضعفين والمكروبين والمظلومين من المسلمين، واكلأهم واحفظهم وأمدهم وتولهم واهدهم ووفقهم لما تحبه وترضاه.

Ya Allah, tunyanyue na utuepushe na Waislamu madhara, balaa, dhulma, kukandamizwa, na kila aina ya dhiki, maradhi, upotofu, upotofu, na ujinga, iwe dhahiri au kwa siri. Ewe Allah Subahanah wa Ta'ala, waokoe wanyonge, walio na dhiki, na waliodhulumiwa miongoni mwa Waislamu. Wape riziki, walinde, waunge mkono, wajali, waongoze, na uwajaalie kufuzu katika yale unayoyapenda na kuyaridhia.

Na mfano mwengine ni kama:

اللهم الطف بنا وبهم فيما يجري به القضاء، واصرف عنا وعنهم شر الطغاة والظلمة والفاسدين ومن عاونهم عاجلا غير آجل في عافية وسلامة يا أرحم الراحمين.

Ya Allah tujaalie sisi na wao kufaulu katika yale yaliyoamrishwa, na utuondolee sisi na wao maovu ya madhalimu, mafisadi, na wanaowasaidia na kuwanusuru. Ewe Allah Subahanah wa Ta'ala, fanya haraka, bila kuchelewa, katika ustawi na usalama kwa njia ya rehema yako, Ewe Mwingi wa kurehemu.

Kwani anasema Shaykh ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: '**Wakati Msiba unapowashukia Waislam iwe ni kutokana na Mashambulizi kutoka kwa Maadui zao, au Ukame, au Maradhi, au Madhara ya Dhahiri au kitu chochote kitakacho sababisha Madhara kwa kwa Waislam basi Waislam hua wanapendekezwa kusoma Qunut katika Sala zao zote**(Al Majmuu)

Kwani kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua Qunut Nazila hua ni yenye kupendekezwa katika Sala zote isipokua katika Salat Al Janaza na Salat Al Idd ambamo hua inakirihisha. Na pia hua inaruhusika katika Sala za Sunna mbali ya kua hua haipendekezwi. Na tunapozungumzia Qunut Nazila kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua ni yenye kupendekezwa si kutokana na Msiba wa Kijamii tu bali pia Msiba wa Mtu mmoja Binafsi.

Na pia hua inapendekezwa si kwa Jamii ya Watu husika tu waliofikwa na Msiba husika, bali pia hua inapendekezwa kwa Waumini wengine waliokua mbali na wale waliokutwa na Msiba husika. Na hii kwa mfano kama vile Msiba unaowakuta Waislam wa Ghaza katika wakati huu basi hua inapendekezwa kwa Waislam waliokua Salam kutokana na msiba huo kwa kua mbali nao wasome Qunut Nazila kwa ajili ya kuwaombea Waislam wenzao hao waliofikwa na msiba huo mbali ya kua Waislam wanaopendekezewa Kusoma Qunut Nazila wako mbali na Waislam walifikwa na Msiba husika.

Ambapo Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na pia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ambao wao wanasema kua Inakubalika na kupendekezwa pia. Na hii ni kwa sababu amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Waumini kwa Umoja wao, kuhurumiana kwao na kukirimiana kwao hua ni sawa na mwili wa Ibn Adam**. **Pale Kiungo kimoja kinapokua kinaumwa basi mwili wote hua ni wenye kuhisi maumivu hayo kutokana na homa ya mwili na kukosa usingizi katika wakati wa Usik**u'*(Sahih Bukhari)*

Hivyo Qunut Nazila kwa Ummah wa Kiislam hua ni Jukumu la Mtu mmoja mmoja na pia Jukumu la Jamii kwa ujumla katika Kusimamia Maslahi ya Kujikinga dhidi ya Maafa na kujijali Kiutu, Kiimani na Kijamii kwa ujumla.

Kwani anasema Shaykh ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: '**Wakati Waislam wanapojaribiwa na Mtihani wa Maangamizo kama Khofu, Njaa, Maradhi ya Maambukizo, Uvamizi wa Wadudu kama Nzige n.k basi Qunut Nazila hua inabidi kusomwa**, **Lakini inapokua Hakuna Msiba basi hua haina haja ya Kusomwa Qunut Nazila.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na pia amesema Mujaddid Ad Din, Mujtahid Imam Abu Abd Allah Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Kama ikiwa kuna Msiba au Mtihani wa Maangamizo, basi hua inaruhusika Kusoma Qunut Nazila hata katika Nyakati ambazo imekatazwa kusoma Qunut ndani yake**. **Kwani ni Makruh Kusoma Qunut katika Salat za Idd Mbili, na Katika Sala ya Kuomba Mvua, lakini kama ikiwa kuna Msiba au Maangamizo, basi hua si Makruh.'***(Al Umm)*

Ama kuhusiana na hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu isemayo* kua:

بَيْنَا النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم يُصَلِّي الْعِشَاءَ إِذْ قَالَ " سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ ". ثُمَّ قَالَ قَبْلَ أَنْ يَسْجُدَ " اللَّهُمَّ نَجِّ عَيَّاشَ بْنَ أَبِي رَبِيعَةَ، اللَّهُمَّ نَجِّ سَلَمَةَ بْنَ هِشَامٍ، اللَّهُمَّ نَجِّ الْوَلِيدَ بْنَ الْوَلِيدِ، اللَّهُمَّ نَجِّ الْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ، اللَّهُمَّ اشْدُدْ وَطْأَتَكَ عَلَى مُضَرَ، اللَّهُمَّ اجْعَلْهَا سِنِينَ كَسِنِي يُوسُفَ

Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua akisali Sala ya Isha alisema: Sami Allahu Liman Hamida! Rabbana wa Laka Al Hamd. **Na kisha kabla ya kuingia kwenhe Sujud basi akasema: Ya Allah waokoe kina Ayash Ibn Rabiah, Ya Allah waokoe kina Salama Ibn Hisham, Ya Allah waokoe kina Al Walid Ibn Walid, Ya Allah waokoe walio dhaifu miongoni mwa Waumini, Ya Allah! ifanye Adhabu yako iwe kali kwa Kabila la Mudar, Ya Allah wanakamishe kwa Miaka ya Ukame kama ilivyokua miaka ya Yusuf.'***(Sahih Bukhari)*

Ambapo anasema Al Hafidh Imam Abu Sulayman Hamd Ibn Muhammad Al Khattabi Al Busti Al Shafii kuhusiana na Hadith hii kua: '**Miongoni mwa Vithibitisho vya Hadith hii ni kuthibitisha kua Inakubalika Kusoma Qunut Nazila katika Sala nyenginezo zaidi ya Salat Al Witr.**

Hadith hii pia inathibitisha kua Kuomba Dua kwa ajili ya Ummah, au Taifa au Watu wengineo kwa Kutaja Majina yao Na majina ya **Mababa zao ndani ya Dua ya Ndani ya Sala hakutoifanya Sala ya Mtu husika kua ni Batili**.

Na pia Inathibitisha kua kuwaombea Adhabu Makafiri na Watu waovu na Madhalimu ndani ya Dua ya Ndani ya Sala hua hakubatilishi Sala ya Mtu husika.'*(Maalim Al Sunnan, Imam Al Khattabi)*

Na akasema tena Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Sharaf An Nawawi kua: '**Qunut hua Inaruhusika katika kila Sala kutokana na Nazila na hivyo hua haisomwi bila ya kuwepo kwa sababu Maalum.'***(Minhaj At Talibin)*

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam Al Muhakkikiin Imam Abu Fadhl Shihab Ad Din Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kuhusiana na Kauli hii ya Imam An Nawawi kua: '**Tunapozungumzia kuhusiana na Matukio ya Nazila basi hii hua haimaniishi kua ni Msiba unaosababisha Madhara kwa Jamii tuu bali pia kwa Mtu mmoja mmoja kwa mfano kama Maradhi ya Maambukizo, au pia Mvua Kubwa sana zenye kusababisha Madhara makubaa sana.'** *(Tuhfah Al Muhtaj)*

Na anasema Imam Mulla Ali Al Qari Al Hanafi katika Al Mirqaat Al Mafatih kua: **'Baada ya Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kutuma Jeshi la kupigana na Musailamah Al Kadhaab na katika vita vya watu wa Ahl Al Kitab basi alikua akisoma Qunut miongoni mwao ni kama ifuatavyo:'**

اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْتَعِينُكَ وَنَسْتَغْفِرُكَ وَنُثْنِي عَلَيْكَ وَلا نَكْفُرُكَ ، وَنُؤْمِنُ بِكَ وَنَخْلَعُ وَنَتْرُكُ مَنْ يَفْجُرُكَ ، اللَّهُمَّ إِيَّاكَ نَعْبُدُ ، وَلَكَ نُصَلِّي وَنَسْجُدُ ، وَإِلَيْكَ نَسْعَى وَنَحْفِدُ ، وَنَرْجُو رَحْمَتَكَ وَنَخَافُ عَذَابَكَ إِنَّ عَذَابَكَ بِالْكُفَّارِ مُلْحَقٌ ، اللَّهُمَّ عَذِّبِ الْكَفَرَةَ ، وَأَلْقِ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ ، وَخَالِفْ بَيْنَ كَلِمِهِمْ ، وَأَنْزِلْ عَلَيْهِمْ رِجْسَكَ وَعَذَابَكَ ، اللَّهُمَّ عَذِّبْ كَفَرَةَ أَهْلِ الْكِتَابِ الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِكَ وَيُكَذِّبُونَ رُسُلَكَ وَيُقَاتِلُونَ أَوْلِيَاءَكَ ، اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ، وَالْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ ، وَأَصْلِحْ ذَاتَ بَيْنِهِمْ وَأَلِّفْ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ ، وَاجْعَلْ فِي قُلُوبِهِمُ الإِيمَانَ وَالْحِكْمَةَ ، وَثَبِّتْهُمْ عَلَى مِلَّةِ رَسُولِكَ ، وَأَوْزِعْهُمْ أَنْ يُوفُوا بِعَهْدِكَ الَّذِي عَاهَدْتَهُمْ عَلَيْهِ ، وَانْصُرْهُمْ عَلَى عَدُوِّكَ وَعَدُوِّهِمْ ، إِلَهَ الْحَقِّ وَاجْعَلْنَا مِنْهُمْ

Ya Allah tunakuomba msaada wako na usamehevu uwako, tunakusifu, lakini hatukukufuru, tunakuamini, na tunamkataa na tunaachana nae kila mwenye kukukufuru.Ya Allah kwako wewe ndiko tunakosujudia, tunakoabudia, tunakoelekea na tunakotegemea kwa rehma zako. Na tunakoogopea Adhabu,kwani kwa hakika Adhabu zako zinashikaman na Wanaokupinga. Hivyo Waadhibu Wanaokukufuru kwa kuwatia Khofu na Upotovu zaidi ndani ya Nyoyo zao, Washushie Mchukizo yako na Adhabu zako, Waliokukufuru miongoni mwa Watu wa Ahl Al Ktab wenye

kuzuia njia yako, na kukataa Mitume wako, na kuwaua Mitume wako. Ya Allah Wasamehe Wenye Kukuamini na upe nguvu umoja wao na ujaze ndani ya Nyoyo zao Imani na Hikma na kua ni wenye kusimamia Imani ya Mtume wako *Salallahu Alayhi wa Salam.* Na wabariki kwa kuana Msimamo katika Imani yao na wasaidie dhidi ya Maadui zao. Ewe Mungu wa haki tujaalie kua ni miongoni mwa wenye kusaidiwa nawe. *(Mirqat Mafatih).*

Kwani anasema Imam Ibn Hajar Al Haytami kua : '**Qunut Nazila hua inasomwa kwa Kila Msiba uwe kwa Muislam mmoja au wengi kulingana na sababu tofauti na aina tofauti za Misiba, kwani kutokana na kua Hadith hazikuainisha kitu juu yake isipokua Dua.**

**Hivyo Wanazuoni wamejumuisha kila kitu ndani yake chenye kusababisha Madhara kwa Waislam kupendekezwa kuondolewa kwa Qunuti ikiwemo kukamatwa kwa Wapiganaji mahiri wa Kiislam. Na hii ni Kulingana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliposoma Qunut Nazila kwa ajili ya watu wa Qurra miongoni mwa Masahaba ambao waliuliwa katika maeneo ya Bir Maunah. Na hii haimaanishi kua kuwaombea Uhai wao wale waliokwishakufa kwa sababu Jambo hilo hua haliwezekani.*(*Tuhfah Al Muhtaj)*

Na Imam Ibn Jariri At Tabari anasema kua: '**Miongoni mwa Sunnah zinazoliwa mkazo kutokana na ubora wake ni ni Kusoma Qunut Nazila katika kila Sala ya Fardhi pale Waislam wanapokua katika Mitihani hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapowapa Ushindi, au atakapojaalia Waislam hao kuwashinda Maadui zao, au Maadui zao hao waingie kwenye Dini ya Kiislam au wajisalimishe kama ilivyotokea katika Msiba wa Bir Al Maunah'***(Tadhib Al Athar)*

Kwani katika wakati wa Kipindi cha Mamlaka ya Utawala wa *Amir Ul Muuminina* Abu Bakr Ibn Al Saddiq *Radhi Allahu Anhu* ambae alitawala kwa mda wa miaka miwili baada ya Kufariki*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Basi Abu Bakr As Siddiq Radhi Allahu alimtuma Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu* kuongoza Jeshi la Kislam kaa ajili ya kupigana vita na Jeshi la Musallama Al Kadhdhab ambae alikua akijiita kua ni Mtume pia.

Na baada ya Kutuma Jeshi hilo basi Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* akawa anasoma Qunut Nazila pia katika wakati huo wa Vita hivyo dhidi ya Musallima.Kama ilivyoelezewa katika Mirqat Al Mafatih na Al Allamah Mulla Al Qarri.

Na katika wakati wa Utawala wa wa Mamlaka ya *Amir ul Muuminin* Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* pia basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* aliwasomea Qunut Wakristo waliokua wakipigana na Waislam pia kama ilivyoelezewa katika Sunan Al Kubra lil Bayhaqi.

Na katika wakati wa Utawala wa wa Mamlaka ya Amir ul Muuminin Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* pia basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* aliwasomea Qunut Wakristo waliokua wakipigana na Waislam pia kama ilivyoelezewa katika Sunan Al Kubra lil Bayhaqi.

Na hivyo anasema Imam Al Shirbini kua:**'Imam anatakiwa akuze sauti yake katika Kisomo cha Qunut Nazila katika Salat Jahriah - Za Sauti (Fajr, Maghrib, Isha na Jumaa) na katika Sirriyah (Dhuhr na Al Asr) lakini kwa upande wa Mtu anaesali peke yake basi anatakiwa asome kimya kimya kama ilivyo kwenye Salat Al Fajr.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Ambapo kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Zakariyyah Al Ansari basi yeye anasema kua:**'Katika Qunut zote za Sala za Sauti na za Kimua kimya basi Imam anatakiwa annayue sauti kwa ajili ya kufuata Sunna ya *Rasul Allah Salallahu AlayhiWa Salam* kama ilivyoelezewa katika Hadith ya Imam Al Bukhari. Na Imam Al Mawardi amesema pia kua: Kupaza Sauti katika Qunut kusiwe**

sawia na Kupaza sauti kwa Kisomo cha Quran katika Sala, na hii si kwa yule anaesali peke yake kwani hatakiwi kupaza sauti.'*(Asna Matalib)*

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Imam kutakiwa Kusoma Qunut kwa Sauti hii ni kwa Sababu Imam ni mwenye Kufuatwa na Maamuma wake na hivyo Maamuma hutakiwa Kuitikia Aamiin Kwa sauti kutokana na Kisomo cha Qunuti hio kwani hivyo ndivyo Alivyofanya R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Masahaba zake.

Na anasema Imam Al Jamal Al Shafii kua:**'Maamuma anatakiwa kuthibitisha Dua ya Imam wake kwa kuitikia kwa sauti, au kumtukuza Allah kwa kimya kimya au kwa kumsikiliza Imam. Kama ilivyosemwa katika Rawdha au Kushuhudiakama ilivyotajwa na Al Mutawali, Ila jambo la Muhimu ni la kwanza kutokana na Uthibitisho wa vitendo vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama ilivyoelezewa na Imam Al Hakim.**

Ambapo mwanzo wa Kumutukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Dua ya Qunut ni mwanzoni mwake. Kama Maamuma atakua anasikia kisomo cha Imam wake, na kama itakua hasikii basi Maamuma anatakiwa asome Qunut yake kimya kimya kama kwenye Dhikr nyengine ndani ya Sala yake.' *(Hashiyyah Al Jamal aala Sharh Al Minhaj)*

Kwa Sababu anasema Imam Sulayman Al Bujairimi Al Shafii kua: '**Sehemu ambazo Maamuma anatakiwa Atamke kwa Sauti Ndani ya Sala ni 4.**
1-Kutikia Amiin baada ya Kisomo cha Surat Al Fatiha.
2-Kuitikia Amiin katika Qunut ya Salat Al Fajr.
3-Kuitikia Amiin katika Qunut ya Salat Al Witr kuanzia Katikati ya mwezi wa Ramadhani.
4 Kuitikia Amiin katika Qunut Nazila ndani ya Sala 5.'*(Hashiyyah Al Bujaraimi)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Al Allamah Ibn Aabidin Ash Shami Al Hanafi kua: '**Qunut Nazila hua inasomwa pale Waislam wanaposhushiwa Msiba,na Hua inaomwa katika Salat Al Fajr baada ya Kurukuu**. **Na hua ni bila ya Kunyanyua Mikono, na pia Mtu hutakiwa kuitikia Amiin kwa sauti ya Chini chini iwe mtu huyo anasali Sala ya Jamaa au Sala ya peke yake**. **Hivyo kama Imam atasoma Qunut katika Salat Al Fajr bila ya kuwepo kwa Msiba, au Mitihani au kama akisoma Qunut Nazila katika nyengineno isiyokua Salat Al Fajr, basi Maamuma hatakiwi kunyanyua Mikono wala Kuitikia Amiin.**

Na hii ni kwa Sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakufanya hivyo. **Kwani Vithibitisho vinaonesha kua Qunut Nazila hua ni Katika Salat Al Fajr tu.'***(Hashiyyah Ibn Abidin)*

Kwani huo ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kuhusiana na Qunut Nazila kama ilivyoelezewa na Imam Ibn Abidin,ambae hata hivyo anaendelea kutuambia kua: '**Hapa inabidi tuwe Makini kuhusiana na pale inapokua Mtu husika anafuata Madhhab gani kutokana na Utofauti wa Mitizamo**. **Hususan pale inapokua hukmu ya jambo husika kua halimaanishi kua ni Makruh katika Madhhab yake anayofuata.'**

Naam..Hivyo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wanasema kua Qunut Nazila inatakiwa isomwe kimya kimya kwa sababu kuna Mitizamo miwili tofauti ndani ya Madhhab hayo kutokana na Hadith ambayo imeelezewa na Imam Ali Shurunbulali ambae anasema kua: '**Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alikua akisoma Qunut Kimya Kimya na baadhi ya wakati alikua akisoma kwa Sauti lakini kwa ajili ya kuwafundisha wale aliokua akiwasalisha.'***(Maraqi Al Falah)*

Hivyo kwa Upande wa Imam Muhammad Ash Shaybani Al Hanafi basi amesema kua Qunut Nazila inatakiwa isomwe kimya kimya, lakini kwa upande wa Imam Abu Yusuf Al Hanafi basi yeye anasema kua inatakiwa isomwe kwa Sauti.

Na katika kuhitimisha kwao baina ya Mitizamo miwili hii basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa waliofuatia wakaamua kufuata Mtizamo wa kua Qunut inayakiwa isomwe Kimya Kimya
Na hivyo ndivyo ilivyoelezwa pia katika Fatawa Al Hindiya, Radd Al Mukhtar n.k.

Na hii pia ni Kulingana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae amesema kua: '**Dua Bora hua ni Hua ya Kimya Kimya.'***(Musnad Imam Ahmad)*

Na pia kulingana na aya isemayo:

﴿ ادْعُواْ رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً إِنَّهُ لاَ يُحِبُّ الْمُعْتَدِينَ﴾

Ud'Aau Rabbakum TadharuaAn wa KhufyatiInnahu La Yuhhibu AlMuAatadiina*(Surat Al Araf 7:55)*

Tafsir ***- Kwa hakika yeye hawapendi wenye Kuvuka Mipaka - Muombeni Mola wenu kwa Unyenyekevu na kwa Siri.***

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Imam Al Buhuti Al Hanbali kua: '**Kusoma Qunut katika Sala isiyokua ni Sala ya Witr hua haiprendekezwi, lakini kama Mtu atakua ni Maamuma Nyuma ya Imam anaesoma Qunut Nazila katika Salat Al Fajr kutokana na Mitihani basi Maamuma anatakiwa aitikie Amiiin.'**

Katika Sala ya Ijumaa Dua ya ndani ya Khutba ya Sala ya Ijumaa hua inatosheleza, kwa hivyo hakuna haja katika Salat Jumaah. **Na pia Sala ya Mtu haitobatilika hata kama Imam atakua ni mwenye kusoma Qunut kutokana na Mitihani.'***(Kashshaf Al Qina-Imam Al Buhuti)*

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik basi hua inapendekezwa kusoma Qunut kimya kimya lakini pia hua inaruhusiwa kusomwa kwa Sauti.

SALAT AN NABII KATIKA QUNUT

❖❖❖❖

Hivyo kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni Kua:**Sala ina Sunan Ab'aadh au Sunnah za Wajib 7 ambazo Mtu akiwacha Moja kati yao basi humbidi kuleta Sijdat Sahw.Ambapo Sunnah hizo ni: Kikao cha Tahiyyat ya Mwanzo kwa Sala yenye Tahiyyat zaidi ya Moja; Kisomo cha Tahiyyat ya mwanzo, Salat An Nabii katika Tahiyyat ya mwanzo**. **Tashahhud kutoa Shahada katika Tahiyyat ya mwanzo, Kusimama katika Kisomo cha Qunut katika Salat Al Fajr, Salat Al Witr ya Nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan**. **Kusoma Qunut katika Sala ya Al Fajir na katika Salat Witr kuanzia nusu ya pili ya mwezi wa Ramadhan.Na Sunnah ya Saba ni Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika mwishoni mwa Kisomo cha Qunu**t*. '(Safinat An Najaa)*

Na ingawa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wameichukulia Salat An Nabii kua ni Sunnah ya Wajib lakini ukweli ni kua Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na *Salat An Nabii Salallahu Alayhi wa Salam* katika kumalizia Kisomo cha Qunut.Kwani Kuna wanaosema kua Haitakiwi kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam***,** na kuna Wasemao kua Inakubalika na inapendekezwa.

Ambapo Miongoni mwa Wanaosema haifai ni pamoja na Imam Abu Qasim Al Safar wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa,Lakini hapo hapokwa upande huo huo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi Imam Abu Al Layth Al Samarqandi tunaona kua yeye anasema kua Inakubalika kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Kumtumia Salam. Ambapo hua pia ndio Mtizamo wa Imam Muhammad Alau Ad Din Al Haskafi Al Hanafi kama alivyosema katika kitabu chake cha Durr Al Mukhtar.

Na pia kwa upande wa Sultan Al Ulamaa Imam Abu Muhammad Izza Ad Din Abd Al Azizi Ibn Abd Salam Ibn Abu Qasim Ibn Hasan Al Sulami Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Na kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Qunut sio Jambo Sahih,kwani haipendekezwi kuongeza kitu chochote kile zaid ya aliyoyasoma *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Sala.'***(Al Fatawa Imam Izz Ad Din)***

Na akasema Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Farra Al Baghawi Al Shafii kua: '**Hairuhusiku Kutuma Salam kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wala Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika mwishoni mwa Dua ya Qunut**. **Hivyo yeyote atakaefanya hivyo basi Sala yake itabatilika kwani anafanya mambo ambayo hayako katika mahala pake.'***(Al Majmuu)*

Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Qadhi Husayn Ibn Ahmad Ibn Muhammad Al Marwazi Al Shafii ambae ni Mwalimu wa Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Farra Al Baghawi Al Shafi.

Kwa maana hio basi katika Madhhab ya Imam Al Shafii kuna Mitizamo miwili tofauti kuhusiana na Salat An Nabii katika Mwishoni mwa kisomo cha Qunut kama vile tulivyoona kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa.Yaani kuna Mtizamo usemao kua Inapendekezwa na kuna usemao hua Haifai.

Hivyo tunarudi kwenye Mtizamo unaotegemewa zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii na kuangalia katika kitabu kiitwacho *Fiqh Al Manhaj aAla Madhhab* Al Imam Al Shafii ambamo imesemwa kua: **Na inapendekezwa zaid kumalizia Qunut kwa kusema:**

فَلَكَ الْحَمْدُ عَلَى مَا قَضَيتَ نَسْتَغْفِرُكَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا وَنَتُوبُ إِلَيكَ وَصَلَّى اللهُ عَلَى سَيدِنَا مُحَمَّدٍ النَّبِيِّ الأُمِّيِّ وَعَلَى آلِهِ وَصَحبِهِ وَسَلَّمَ

***Falaka Al Hamd Aala Ma Qadhayt* - Hivyo Shukran zote ni juu yako kwa kila unachokikadiria.**
***Nastaghfirruka Allahuma Rabbana Wanatubu Ilayka* - Tunaomba Msamaha Wako ewe Mola wetu na Tunatubu kwako.**

Wasala Allahu aAla Sayyidna Muhammad Al Nabiyyi Al Umiyyi wa aAla Alihi wasahbihi Wasalam* - Na Sala na Salam za Allah ziwe juu ya Bwana wetu *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* Mtume asiejua Kusoma na juu ya Familia yake na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum.*(Fiqh Al Manhaj)***

Naam..huu ndio Mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii na Wanazuoni waliobakia wa Madhhab ya Imam Al Shafii na kua ndio *Qawl Al Mutammad* yaani Kauli inayotegemewa ya Madhhab ya Imam Al Shafii na pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.Na Msingi wa Mtizamo huu ni wenye kusimamia kwenye Hadith iliyomo kwenye Sunnan An Nasai ambayo inasema:

أخبرنا محمد بن سلمة قال حدثنا ابن وهب عن يحيى بن عبدالله بن سالم عن موسى بن عقبة عن عبدالله بن علي عن الحسن بن علي قال: علمني رسول الله – صلى الله عليه وسلم – هؤلاء الكلمات في الوتر قال: (قل: اللهم اهدني فيمن هديت و بارك لي فيما أعطيت و تولني فيمن توليت و قني شر ما قضيت فإنك تقضي و لا يقضى عليك و إنه لا يذل من واليت تباركت ربنا و تعاليت و صلى الله على النبي محمد

Amesema Muhammad Ibn Salamah kua amesema Ibn Wahb kua amesema Yahya Ibn Abd Allah Ibn Salim kua amesema Musa Ibn Uqbah kua amesema Abd Allah Ibn Ali kua amesema Al Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alinifundisha mimi maneno yafuatayo katika Salat Al Witr:

***Allahuma Ihdini Fii Man Hadayt* - Ya Allah Niongoze Kama Ulivyowaongoza Waliongoka**.
***Waafini Fiiman aAafayt* - Na Niokoe kama Ulivyowaokoa Waliokoka.**
***Watawalani Fiiman Tawalayh* - Na Nisimamie kua miongoni mwa Uliowasimamia.**
***Wabarik Fiiman A'atayt* - Na Nibariki Katika Ulichonipa**
***Waqinni Sharran Ma Qadhait* - Na Nikinge na Shari Ulizoniandikia zinifike.**
***Innaka Taqdhi wala Yuqdha Aalayk* - Kwa Hakika wewe ndie Mwenye Kutaka Na Hakuna Anaeweza kutaka Dhidi yako.**
***Wainnahu la Yadhilu Man Walayt* - Na kwa Hakika Hadhaliliki Yule Ulie karibu nae.**
***Wala YaiI'zu Man Adayt* - Na Wala Hatukuki Alie Adui Yako.**
***Tabarakta Rabbana Wa TaA'alayt* - Baraka zote ni Zako Ewe Mola wetu na Utukufu ni wako.**
Wasala Allahu aAla Nabii Muhammad* - Na Sala za Allah Zimfikie Nabii Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam(Sunan An Nasai)*

Hivyo amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii ya Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* inayozungumzia Qunut yenye kumalizia na maneno yasemayo:

Wasala Allahu aAla Nabii Muhammad* - Na Sala za Allah zimfikie Nabii Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam.' *(Sunan* An Nasai)

Kua: '**Na Ushahidi wa Skuli ya Madhhab yetu (Madhhab ya Imam Al Shafii) kua ni yenye kupendekezwa kumsalia na Kumtumia Salam *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Qunut, ni kutokana na Nukuu ya Hasan Ibn Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alinifundisha mimi maneno haya kwenye Salat Al Witr'**

Akasema *Allahuma Ihdini fii man hadayt,* na akatamka sentensi nane na kisha akasema mwishoni mwake kua: 'Wasala Allahu aAla Nabii Muhammad - Na Sala za Allah Zimfikie Nabii *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam.''*

Na haya ndio maneno aliyoyanukuu Imam An Nasai kupitia katika Hadith yenye Mnyororo mzuri wa walionukuu.*'(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Na ingawa Mujaddid Ad Din Al Hafidh Imam Shihab Ad Din Abu Fadhl Ibn Hajar Al Asqallani amesema katika Talkhis kuhusiana na hadith hii kua:**'Hii Hadith ni Munkar kwa sababu Abd Allah Ibn Ali ni Mtoto wa Husayn Ibn Ali ambae hakukutana na Hasan Ibn Ali, na kuna kutokukubaliana kuhusiana na Musa Ibn Uqba katika Kunuu kwake.'**

Ambapo maneno haya ni yenye kuifanya hadith hii kua ni yenye kasoro ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Al Hafidh Imam Ahmad Ibn Muhammad Al Qastallani Al Shafii na pia ndio Mtizamo wa Al Hafidh Imam Muhammad Al Zarqani Al Maliki n.k.

Lakini hata hivyo tunapoangalia Hadith za Masahaba *Radhi Allahu Anhum*akiwemo Sahaba Mwanazuoni Ubbay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu*, basi alikua akimsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mwishoni mwa Kisomo chake cha Qunut. Kama ilivyoelezewa na Imam Ibn Khuzaymah katika Sahih yake.

Na pia Abu Halima Muadh Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua akisalisha kama Imam mbadala wa Ubbay Ibn Kaab *Radhi Allahu Anhu* katika wakati wa Utawala wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kama ilivyonukuliwa na Imam Ismail Ibn Is-aq Al Qadhi kua alikua Abu Halima alikua akimalizia Qunut kwa Sala na Salam kwa *Nabii Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na Sala na *Salam kwa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi amesema Imam Al Mardawi Al Hanbali kua: **'Na baada ya Kumaliza Kusoma Qunut basi inatakiwa Kutuma Salam kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salaam,* na huu ndio Mtizamo wa Madhhab yetu'***(Al Insaaf)*

Na Imam Ibn Al Qayyim Al Jawziyyah nae katika kuelezea sehemu zinazopendekezwa kutuma Sala na Salam kwa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua: '**Inapendekezwa pia Kutuma Salam kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mwishoni mwa Dua ya Qunut kama alivyopendekeza Imam Al Shafii na wale waliokubaliana nae.***(Al Jalaa Al Afham)*

Kwani anasema Imam Shams Ad Din Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini Al Shafii kua:
Kuhitimisha Qunut kwa maneno yasemayo:

فَلَكَ الحَمْدُ عَلَى مَا قَضَيْتَ، نَسْتَغْفِرُكَ اللَّهُمَّ رَبَنَا وَنَتُوْبُ إِلَيْكَ، وَصَلَّى اللهُ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّدٍ النَّبِيِّ الأُمِّي وَعَلَى آلِهِ وَصَحْبِهِ وَسَلَّمْ.

Falaka Al Hamd Aala Ma Qadhayt - Hivyo Shukran zote ni juu yako kwa kila unachokikadiria Nastaghfirruka Allahuma Rabbana Wanatubu Ilayka - Tunaomba Msamaha ewe Mola wetu na Tunatubu kwako.

Wasala Allahu aAla Sayyidna Muhammad Al Nabiyyi Al Umiyyi wa aAla Alihi wasahbihi Wasalam - Na Sala na Salam za Allah ziwe juu ya Bwana wetu *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* Mtu asiejua Kusoma na juu ya Familia yake na Masahaba zake Radhi Allahu Anhum

Ni kwenye kupendekezwa kutokana na Msingi wa Vithibitisho vya Hadith Sahih, **Tofauti kuhusiana na Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya kuomba Dua na baada ya kufanya Dhikr.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Kwani Kumsalia Na kumtumia *Salam Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m hua hakupendekezwi katika Siku ya Ijumaa tu na Kwenye Kuomba Dua ikiwemo Dua ya Qunut bali pia Hua inapendekezwa Kufanya hivyo katika Kila wakati ambao Mtu unapokua na nafasi. Lakini pia Wanazuoni wanapendekeza zaid katika Nyakati zifuatazo:

Katika Usiku na Mchana wa Siku ya Al Khamis,Ijumaa na Jumamosi na Jumapili, kama ilivyothibitishwa katika Hadith mbali mbali tofauti.
Katika Wakati wa Baada ya Salat Al Fajr na Magharibi.
Katika Wakati wa Kuingia Msikitini na katika Wakati wa Kutoka.
Katika Wakati wa Kutembelea Kaburi la Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.
Katika wakati wa Sai au kutembea kwa haraka haraka baina ya Safa na Marwa.
Katika Khutba za Sala na Khutba za Haja kama Harusi n.k.
Kabla na Baada ya Kusomwa Adhana na Iqamah.
Mwanzoni Katikati au mwishoni mwa kisomo cha Dua yeyote.
Baada ya Kisomo cha Qunut.
Baada ya Kumaliza Talbiyyah.
Baada ya Kutia Udhu.
Baada ya kukutana na kuagana.
Unaposahau Kitu.
Mnapousiana Mema na kukatazana maovu.
Unapotoa Fatwa.
Unapomaliza kusoma Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*
Na katika kila Jambo Muhimu la kheri isipokua unapokua Chooni au Inapokua Wanandoa mnaingiliana kimwili.

SUNNAN HAI'AT

❖❖❖❖

Kwani baada ya kuangalia Sunnah Ab'aadh basi tunaangalia kuhusiana na Sunnah za Sala ambazo si Wajib bali hua ni Sunnah kama Sunah na hivyo hujulikana pia kama Sunnan Hai'at

Na hivyo kwa kua ni Sunnah kama Sunnah basi Sunnan Haiat hua hazihitaji Sijdat Sahw kama zikiachwa kwa Makusudi au kwa kusahauliwa.

Na kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua hua kuna Tofauti kuu 4 baina ya Sunnan Ab'aadh na Sunnan Haiat ambazo ni:

1-Sunnan Ab'adh ukiiwacha basi inabidi ulete Sijdat Sahw lakini Ukiiwacha Sunnan Haiat basi haina haja kuleta Sijda Sahw.

2-Sunnah Ab'aadh Hua ni Sunna zinazojitegemea na hivyo hua hazijumuishiki na Nguzo za Sala, kwa mfano Tahiyyat ya kwanza na Qunut Ambapo vitendo vyote hivi hua vinajitegemea

Lakini Sunnan Haiat hua Zinashikamana na Nguzo za Sala, kwa Mfano Dhikr Allah na Tasbih ambazo huenda sambamba na Nguzo za Rukuu au Sujud

3-Sunnan Ab'adh hua zina seheme zake Maalum kama tunavyoona kwenye Tahiyyat na Qunut wakati Sunnah Haiat hazina sehemu Maalum bali zinaambatana na Nguzo za Sala

4-Sunnan Ab'aadh hua haipendekezwi kufanywa nje ya Sala Wakati Sunnan Haiat hua Zinapendekezwa pia kufanywa ndani ya Sala na nje ya Sala kwa mfano Tasbih, Dhikr n.k

Naam Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wamezigawa Sunna za Sala zijulikanazo kama Sunnan Haiat katika Makundi mawili yafuatayo:

1-Sunnah Qawliyah - Sunna za Kauli au Maneno.

2-Sunnah Fii'liyyah - Sunnah za Vitendo.

Hivyo tunaanza na Sunnah za Kauli ambazo ni zifuatazo:

1- Kusoma Dua ya Iftitah yaani Dua ya Ufunguzi wa Sala kwa Sauti ya Chini chini kimya kimya, ambapo miongoni mwa mifano ya Dua hio ni:

اللهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا وَالْحَمْدُ لِلهِ كَثِيْرًا وَسُبْحَانَ اللهِ بُكْرَةً وَاَصِيْلًاوَجَّهْتُ وَجْهِي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضَ حَنِيفًا، وَما أَنَا مِنَ المشْرِكِينَ، إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي، وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ العَالَمِينَ، لا شَرِيكَ له، وَبِذلكَ أُمِرْتُ وَأَنَا مِنَ المسْلِمِينَ،

Allahu Akbar Kabira W Alhamdulillaahi Kathiiraa, wa Subhaan Allahi Bukratan Wa'asillaa, Inni Wajjahtu Wajhiya lilladhi Fattara Samaawaati wal Ardha Haniifan Musliman wamaa Anaa Minal Mushrikiin. Inna Ssalaati wa Nusuki wa Mahyaaya wa Mamaati Lillahi Rabbil 'aalamiin. Laa Sharikalahu wa Bidhaalika Umirtu wa Ana Minal Muslimiin.

Tafsir: **Allahu Ndie Mkubwa zaidi, Shukran zote zinastahiki kwa Allah Na Utukufu ni wa kwake Asubuhi na Jioni. Kwa Hakika Mimi nnauelekezea Uso wangu kwa Allah, ambae ndie alieumba Mbingu na Ardhi ambavyo vyote ni vyenye utiifu na kujisalimisha juu yake. Na mimi si miongoni mwa wale wanaomshirikisha nae *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kwani Kwa Hakika Sala zangu, Ibada zangu, Maisha yangu, Mauti Yangu ni kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* tu. Ambae ni Mola wa Ulimwengu wote asiekua na Mshirika, Na hivyo ndivyo nilivyoamrishwa kufanya, na Mimi ni Miongoni mwa Waislam (waliojisalimisha kwake *Allah Subhanah wa Ta'ala*).**

2-Kusoma Taawidh yaani Audhu Bi Allahi Minna Al Shaytani Rajim kimya kimya Kabla ya kusoma Kisomo cha Qur'an katika Kila Rakaa, lakini inatilia kazoo Zaidi katika Rakaa ya kwanza

((أَعُوضُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ))

Kwani kama alivyosema Imam An Nawawi kua: 'Taawudh imeamrishwa katika Rakaa ya kwanza , hivyo kama haikusomwa kwenye Rakaa ya kwanza basi inatakiwa isomwe kwenye Rakaa Ya Pili, na kama iksomwakweye Rakaa ya kwanza basi kwenye Rakaa ya pili hua ni

Sunnah tu iliyodhibitishwa lakini kuisoma kwenye Rakaa ya Kwanza hupendekezwa zaidi'*(Al Adhkar)*

3-Kuitikia Amiin baada ya Kisomo cha Surat Al Fatiha.

4-Kusoma Sura nyengineyo baada ya Kusoma Surat Al Fatiha katika Rakaa ya kwanza na katika Rakaa ya Pili.Kwa Kuanzia Aya zisizopunga Tatu Fupi fupi au pia unaweza kusoma Aya moja Ndefu yenye Sentensi zisizopungua Tatu 3 ndani yake kwa mfano Aya Al Kur Sh.

5-Kusoma Surat Al Fatiha na Kisomo cha Sura nyenginezo Kimya Kimya Katika Sala ya Kimya Kimya kama katika Salat Adh Dhuhr na Salat Al Asr na Kusoma kwa Sauti katika Sala za Sauti kama Salat Al Fajr, Maghrib na Salat Al Isha, na Salat Al Jumaa.

6-Kurefusha Kisomo cha Sura baada ya Surat Al Fatiha Katika Rakaa ya kwanza na Kufupisha Kisomo cha Sura ya Pili katika Rakaa ya pili.

Kwa Mfano kama Katika Rakaa ya kwanza Utakua Umesoma Surat Al Ikhlas ambayo ni yenye aya 5 ikiwemo Bismi Allahi Rahmani Rahim.Basi hua ni Sunna katika Rakaa ya pili kusoma Surat Al Kawthar yenye Aya 4 pamoja na Bismi Allahi Rahmani Rahim n.k.

7-Kusoma Takbirat Al Intiqal yaani Kusema Allahu Akbar katika Kila **hatua yenye Nguzo ya Sala kuashiria mabadiliko ya Hatua ya Nguzo Ndani ya Sala Husika, isipokua katika Itidal yaani kutoka katika Hatua ya Nguzo ya Rukuu Kusimama kabla ya kuingia kwenye Hatua ya Nguzo ya Sujud.**

8-Kutamka Tasmii yaani kusema Sami Allahu Liman Hamida, Rabbana wa Laka Al Hamd wakati unapoingia kwenye Itidal.

9-Kufanya Tasbih yaani Subhanah Rabbi Al Aadhim wa Bihamdihi zaidi ya mara moja katika kila Kurukuu.

10-Kufanya Tasbih yaani kusema Subhanah Rabbi Al Aala Wabihamdihi zaidi ya mara moja katika kila Sujud.

11-Kusema Rabbi Ighfirli zaidi ya mara moja Baina ya Sijda mbili.

12-Kuomba Dua katika Tahiyyat ya mwisho kabla ya kutoa Salam.

Hivyo kuhusiana na Sunnah hizi basi hua ni Kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Sunnah zisizokua na sifa ya Ab'aadh (za wajib) kama vile Taawudh(Kusema Audhu Bi Allahi Minna Al shaytani Al Rajim), Dua ya Iftitah (ya Kufungulia Sala), Kunyanyua Mikono katika Kusema Allahu Akbar) Kusema Allahu Akbar**, **Kutamka Tasbih(Subhanah Rabbi Al Adhiim wabihamdihi, Subhanah Rabbi Al Aala Wabihamdihi) katika Rukuu na Sujud, Kusoma Qur'an Kimya Kimya na kwa Sauti, Kuomba Dua, Kukaa Mkao wa Tawwaruk katika Tahiyyat ya mwisho, kukaa mkao wa Iftitash katika Tahiyyat ya mwanzo, Kusoma Sura nyengine baada ya Surat Al Fatiha, Kuweka Mikono kwenye Magoti katika Rukuu, Kutamka Takbir za ziada katika Sala ya Iddna Sunna nyenginezo za Haiat Basi hua hakuna haja ya kuleta Sijdat Sahw kama Mtu ataziacha Kuzitamka, iwe kwa Makusudi au kwa kughafilika nazo.**

Na hii ni kwa sababu hakuna Uthibitisho juu yake kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alileta Sijdat Sahw kutokana na kuzisahau Sunnah hizo tulizozitaja. **Na kutokana na kua Sijdat Sahw hua ni sehemu ya Sala kutokana na Jambo Maalum basi hua haikubaliki kuileta Sijda Sahw juu ya jambo lisilohitajika Kuliletea Sijdat Sahw.'***(Al Majmuu)*

Ambapo amesema Imam Ibn Abi Shaybah katika Musannaf yake kua:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ عَيَّاشٍ، عَنِ الْأَعْمَشِ، عَنْ إِبْرَاهِيمَ، قَالَ: إِذَا أَرَادَ أَنْ يَقُولَ سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَهُ فَقَالَ اللَّهُ أَكْبَرُ فَلَا سَهْوَ عَلَيْهِ

'**Amesema Abu Bakr Ibn Ayyash kua amesema Ibrahim an Nakhai kua: Pale Mtu inapotakiwa kusema Sami Allahu Liman Hamida lakini hata hivyo yeye akasema Allahu Akbar basi hua haihitajiki kuleta Sijdat Sahw juu yak**e.'*(Musanaf Ibn Shaybah)*

Na akasema Imam An Nawawi kua: '**Visomo vya Tasbih, na dhikr nyenginezo ikiwemo za Rukuu na za Sujud na maneno Sami Allahu Liman Hamida na Takbir isiyokua Takbirat Al Ihram hua ni Sunnah na wala si Wajibu.**

Hivyo kama Mtu akiwacha kutamka basi hua hapati dhambi na Sala yake haibatiliki bali hua Sahih, iwe amewacha kutamka maneno hayo kwa makusudi au kwa kusahau. **Ila hua haipendekezwi kwa Mtu kwa makusudi kutotamka maneno hay**o.'*(Al Majmuu)*

Na amesema Imam Sulayman Al Bujaraimi Al Shafii kua: '**Kama Mtu atakua ni mwenye kubadilisha Kutamka maneno ya Sunnah za Haiat katika sehemu ambayo si yake,basi hua haihitajiki kwake kuleta Sijda Sahw isipokua pale itakapokua amesoma Sura ambayo si Surat Al Fatiha katika sehemu ambayo si ya Kisimamo.'** *(Hashiya Al Bujaraimi)*

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Al Jaawi Al Shafi katika Nihayat Al Zayn, Imam Sulayman Al Jamal katika Hashiyyah Al Jamal n.k

Na Kama tulivyosema kua Miongoni mwa Sunnah A Haiat ni*Kusoma Surat Al Fatiha na Kisomo cha Sura nyenginezo Kimya Kimya Katika Sala ya Kimya Kimya kama katika Salat Adh Dhuhr na Salat Al Asr na Kusoma kwa Sauti katika Sala za Sauti kama Salat Al Fajr, Maghrib na Salat Al Isha, na Salat Al Jumaa.*

Na hii nikama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Na hua ni Sunnah kusoma Surat Al Fatiha na Sura inayofuatia Kimya Kimya ndani ya Sala ya Kimya Kimya kama vile**. **Salat Adh Dhuhr na Salat Al Asr, na katika Rakaa ya Tatu ya Salat Al Maghrib na Rakaa ya Tatu na ya Nne katika Salat Al Isha,na hii ni Kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni wote kulingana na Vithibitisho vya Hadith Sahih zenye kuelezea hay**a(*Al Majmuu)*

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Hata kwa Upande wa Mtu anaesali Peke yake katika Sala ya Sauti basi hua ni Sunnah kwake kutoa Sauti kwa Mtizamo wa Upande wa Madhhab yetu ya Al Shafii na pia kwa Jamhuria.'***(Al Majmuu)*

Na kwa kua Kutoa Sauti katika Kisomo cha Qur'an katika Sala ya Sauti hua ni Sunnah basi kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii kama itatokea kwa Mfano Imam anasalisha Sala ya Kutoa Sauti kama Al Fajr, Maghrib, Isha n.k. Kisha akasoma Al Fatiha kwa Sauti lakini akasahau kuhusiana Kusoma Sura

inayofuatia kwa Sauti, au akasahau Kusoma Surat Al Fatiha kwa Sauti na akasoma kimya kimya badala yake, n.k.

Na ikafikia hali ya kua ni mwenye kuingia kwenye Rukuu na Kurukuu na hapo akakumbuka kua kumbe Surat Al Fatiha amesoma lakini si kwa sauti. Basi katika hali kama hii kwa kua ameshaingia katika hatua ya Nguzo nyengine ya Sala basi hua haina Haja kurudia Hatua hio wala Rakaa hio, na Sala yake itakua Sahih.

Lakini kama iikiwa amekumbuka kua kumbe hakusoma kwa Sauti kabla ya kuingia kwenye Rukuu basi hapa itambidi Imam husika kurudia kisomo chake hicho upya kwa sauti.(kama ilivyoelezewa katika *Hashiyyah Al Adawi aAla Sharh Al Khurashi Al Shafii)*

Ama kuhusiana na Sunnah Haiat ya Kusoma Kisomo cha Aya zisizopungua Tatu baada ya Surat Al Fatiha katika Mbili za mwanzoni za Sala, basi anasema Al Khatib Imam Al Shirbini kua: '**Kusoma Sura baada ya Surat Al Fatiha katika Rakaa mbili za Mwanzoni za Sala hua ni Sunna hata kama Sura hio ikiwa ni ndogo**, **Iwe katika Sala ya Sauti au Sala ya Kimya Kimya**. **Ama kuhusiana na Maamuma basi hua si Sunnah kwake yeye Kusoma Sura baada ya Surat Al FatihaBali anatakiwa akae kimya huku akisikiliza Kisomo cha Sura anayosoma Imam.'***(Al Iqna Fi Hili Al Faz Abu Shujaa)*

Kwa maana hio basi Kusoma Sura nyengine baada ya Surat Al Fatiha katika Rakaa mbili za mwanzo za Sala yeyote hua ni Sunnah kwa Mtu anaesali peke yake na pia kwa Imam anaesalisha wengine.Lakini hua si Sunnah kwa Maamuma.

Na kwa kua Kufanya hivyo hua ni Sunnah basi hukmu yake kwa asiesoma hua ni kama alivyosema Imam An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Sunnah zisizokua Ab'aadh basi hua haina haja kuiletea Sijdat Sahw pale inaposahauliwa au inapoachwa kwa Makusudi, na huu ndio Mtizamo Sahih unaojulikan**a.'*(Rawdha Talibin)*

Kwani tulisema kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wamezigawa Sunna za Sala zijulikanazo kama Sunnan Haiat katika Makundi mawili yafuatayo:

1-*Sunnah Qawliyah* - Sunna za Kauli au Maneno

2-*Sunnah Fii'liyyah* - Sunnah za Vitendo

Na Alhamd lillah tumeangalia kuhusiana na *Sunnah Qawliyyah,* hivyo tunaingia katika *Sunnan Fiiliyyah* ambazo ni Sunnah za Vitendo nazo ni:

1-Kunyanyua Mikono katika wakati wa Takbirat Al Ihram, yaani Takbir ya Kuingilia ndani ya Sala.

Ambapo Mikono hunyanyuliwa hadi kwenye usawa wa Mabega ama zaidi hadi juu ya mabega karibu na Masikio huku Matumbo ya Viganja yakiwa ni yenye Kuelekezwa katika Upande wa Kibla.

2-Kunyanyua Mikono hadi Usawa wa Mabega au Juu zaid karibu na Masikio katika wakati wa kuingia kwenye Kurukuu.

3-Kunyanyua Mikono hadi Usawa wa Mabega au juu zaidi hadi karibu na Masikio katika wakati wa Kutoka kwenye Rukuu, na pia katika wakati wa kutoka kwenye Sujud baada ya Rakaa ya pili kuingia kwenye Rakaa ya Tatu.

Kwani Imam Al Bukhari anasema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:

رَأَيْتُ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا قَامَ فِي الصَّلاَةِ رَفَعَ يَدَيْهِ حَتَّى يَكُونَا حَذْوَ مَنْكِبَيْهِ، وَكَانَ يَفْعَلُ ذَلِكَ حِيْنَ يُكَبِّرُ لِلرُّكُوعِ، وَيَفْعَلُ ذَلِكَ إِذَا رَفَعَ رَأْسَهُ مِنَ الرُّكُوعِ

(رواه البخاري)

Mimi nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika wakati ambao alipokua akinyanyuka katika Sala alikua akaisnyanyua mikono, hadi kufikia kwenye usawa wa Mabega yake. Na alifanyahivyo pia alipokua akiingia katika Rukuu na akinyanyuka kutoka katika Takbir ya Rukuu. Na alikua akifanya

Na imenukuliwa kwa *Nafii Radhi Allahu Anhu* kua: 'Abd Allah Ibn Umar*Radhi Allahu Anhu*alikua akinyanyua mikono yake katika wakati wa kunyanyuka kutoka katika Rakaa ya pili, ambapo kitendo hichokilikua ni chenye kutokana na kufuata afanyavyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'*

Na kulingana na mtizamo wa Imam Al Shafii basi ni kua: 'Hikma iliyomo ndani yakunyanyua mikono katika Takbirat Al Ihram, kabla ya kurukuu na baada kurukuu, na baada ya kunyanyka kutoka katika Tahiyyat ya kwanza hua ni kumtukuza *Allahu Subhanah w Ta'ala*, kumuomba malipo kutoka kwake na kufuata *Sunna za Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam*.'

Ama kulingana na Mtizamo wa Sayyid Muhammad Al Jurdani basi yeye anasema kua: 'Hikma iliyomo katika Kunyanyua Mikono katika Hatua za Sala hua ni kuachana na kurembea Vyote vile visivyohusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*'

4-Kuishusha Mikono katika Hatua zote tulizozitaja katika kuinyanyua kwake.

5-Kuweka Mkono wa Kulia juu ya Mkono wa Kushoto baina ya Tumbo na Kifua, kwa aidha Kiganja cha Mkono wa Kulia kukaa juu ya anzio la Kiganja cha Kushoto huku vidole vyake vikiwa vimenyooka, au kwa Kiganja cha Mkono wa Kulia kuishika sehemu iliyoanzia kiganja cha Mkono wa Kushoto.

Na hii ni kutokana na Hadith isemayo kua:

كَانَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَضَعُ يَدَهُ الْيُمْنَى عَلَى يَدِهِ الْيُسْرَى ثُمَّ يَشُدُّ بَيْنَهُمَا عَلَى صَدْرِهِ، وَهُوَ فِي الصَّلاَةِ

Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alikua akiweka mkono wake wa Kulia juu ya mkoo wake wa kushoto na kuikumbatia kwenye kifua chake katika wakati alipokua akisali.(Sunnan Abu Daud)*

Hivyo hua ni Sunna kwa mikono yote kuwekwa kwenye upande wa kushoto wa Kifua, kwani Hikma yake kitendo hicho hua ni kuasehemu hio ndio inayokaa sehemu tukufu ya Moyo wa Ibn Adam na hivyo kuwea mikono katika sehemu hio hua ni kwenye kuashiria ka Mtu husika anailinda Imani yake ndani ya Moyo wake, na hii ni kwa sababu pale mtu anapokua anakitnza kitu au anapokihifadhi hua ni mwenye kutumia mikono yote miwili kwenye kitu husika.

Ambapo Sunna hii hua ni katika wakati wa Kuingia katika Sala baada ya Takbirat Al Ihram na kuishia katika Hatua ya kuingia kwenye Rukuu, na kurudiwa tena katika Kisimamo cha Kila Rakaa inayofuatia.

Ambapo Tukio hili hua Kamwe halitakiwi kufanywa baada ya Kurukuu katika Kisimamo cha Kutoka kwenye Rukuu kuingia kwenye Sijda.

6-Kuelekeza ambacho chini kwa Kuangalia katika Sehemu ya Kusujudia katika wakati wote wa Sala.

7-Kusimama Bila ya Kuibana Sana Miguu na bila ya Kutanua sana miguu.

8-Kushika Magoti huku vidole vya mikono vikiwa vimetawanyika katika wakati wa Kurukuu.

9-Kugusisha Viungo saba vya Mwili vya kusujudia Ardhini katika wakati wa Kusujudu.

10-Kuweka Ardhini viganja Mikono katika usawa wa Mabega, Kutogusisha Visugudi vya mikono na mbavu zako, Kutogusisha Tumbo na Mapaja yako, kutogusisha Mapaja na Misuli ya Miguu, kutogusisha Mapaja pamoja, Kutolaza Nyayo, na kupinda na kuelekeza Vidole vya Miguu katika upande wa KiblaKatika wakati wa Kusujdu.

11-Kukaa Mkao wa Iftirash baina ya Sijda mbili na katika Tahiyat ya kwanza kukaa mkao wa Tawwarruk katika Tahiyyat ya Mwisho.

12-Kuweka Viganja vya Mikono Mwishoni mwa Mapaja karibu na Magoti kwenye kikao cha baina ya Sijda mbili na katika Kisomo cha Tahiyyat na kunyoosha Kidole cha Shahada katika Wakati wa Kushuhudia ndani ya Tahiyyat.

13-Kigeukia upande wa Kulia na Kushoto katika wakati wa kutoa Salam ya Kumalizia Sala.

Na tunapoangalia kuhusiana na Vitendo vya Sunnan za Mapumziko baina ndani ya Sala nzima basi tunaona kua kuna Mapumziko ya utulivu unaotakiwa kupatikana katika sehemu 6 Sita zifuatazo ndani ya Kila Sala ya Mtu husika, ambapo Pumziko hilo Hua ni lenye kutakiwa kuchukua Mda wa kiasi ya kufanya Tasbih yaani kusema *Subhanah Allah.*: Ambapo sehemu hizo za Mapumziko ni kama Ifuayavyo:

1- Utulivu na Baina ya Takbirat Al Ihram na Duat Al Istiftah yaani Dua ya Ufunguzi wa Sala.

2- Utulivu na Baina ya Dua ya Ufunguzi wa Sala na Taawudh yaani Kusema Audhu Bi Allahi Mina Al Shaytani Rajiim kabla ya Kuingia kwenye Bismi Allahi Rahmani Rahiim kwa ajili ya Kusoma Surat Al Fatiha.

3- Utulivu na Pumziko na Utulivu Baina ya Taawudh na Kisomo cha Surat Al Fatiha.

4-Utulivu na Pumziko baina ya Kumalizika kwa Kisomo cha Surat Al Fatiha na Kuitikia Maombi ya Dua ya Surat Al Fatiha kwa neno Amiin.

5-Utulivu na Pumziko baina ya Itikio la Amiin linalotokana na kisomo cha Dua ya Surat Al Fatiha na kabla ya Kusoma Sura Nyengineyo katika Rakaa Mbili za Mwanzoni mwa Rakaa za Kila Sala.

6-Utulivu na Pumziko la baina ya Kumalizika kwa Kisomo cha Sura Inayofuatia baada ya Surat Al Fatiha na kabla ya kuingia kwenye Rukuu.

Kwani tunapoangalia Vituo hivi vya Mapumziko basi mara nyingi hua tunaona kua kuna baadhi ya Maiamamu wanaposalisha hua hawavitilii maanani vituo hivi vya Mapumziko mafupi.Kiasi ya kua Unakuta Imam anasalisha Sala ya Jamaa na kisha baada ya Kusoma Surat Al Fatiha kwa sauti katika Sala ya Sauti,basi mara tu baada ya Maamuma wake kumaliza kuitikia Amiin.

Basi Imam husika huanza na kisomo cha Surat Al Fatiha na hivyo kuwakosesha Maamuma wake mda wa Kusoma Surat Al Fatiha.

Jambo ambalo hua si sahih kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambao wao wanatakiwa Kusoma Surat Al Fatiha kwa kila mmoja wao, iwe Imam au Maamuma. Kwani Surat Al Fatiha ni Nguzo ya Sala kwa kila Mtu.

Na tulisema kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wamezigawa Sunna za Sala zijulikanazo kama Sunnan Haiat katika Makundi mawili yafuatayo:

1-Sunnah Qawliyah - Sunna za Kauli au Maneno.

2-Sunnah Fii'liyyah - Sunnah za Vitendo.

Lakini hata hivyo kuna Watu ambao ni viziwi, na kuna ambao ni Mababu na kuna wenye Maradhi labda ya Vidonda vya Mdomo au Ulimi,hivyo jee Hukmu yao watu kama hawa kwenye Sala katika sehemu za Kauli hua inakuaje?

Kwani amesema Imam Sulayman Al Bujaraimi kua: **Tunapozungumzia Nguzo za kauli ambazo ni Takbirat Al Ihram, Kisomo cha Surat Al Fatiha, Kisomo cha Tahiyyat ya Mwisho, Salat An Nabii Katika Tahiyyat ya Mwisho na Salam ya Kutokea nje ya Sala.**

Ambapo hapa katika Sunna za Kauli kuna Suali ambalo inabidi tulitupie macho kidogo kwani ni lenye kuhusiana na Nguzo za Sala za Kauli na pia Sunnah za Sala za Kauli.

Yaani vitendo vya Sala vinavyotekelezwa na Ulimi kwa Kusema iwe Takbir Al Ihram, Surat Al Fatiha, Sura Nyenginezo,Tasbih, Dhikr, Tahiyyat n.k

Ambapo kama tulivyoona kua Miongoni mwa Masharti yake ni kua Mtu anatakiwa ayatamke Maneno husika ya Sala kiasi ya kuyasikia ndani ya Masikio yake.. Hua zinahitajiwa Kusomwa na Kutamkwa kiasi ya kua ni zenye kutoa Sauti ambayo ni yenye kusikikana na Mtu anaesali ndani ya Masikio yake*(Hashiyyah Al Bujaraimi ala Sharh Minhaj Tulab)*

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi nae amesema kua: '**Sharti la Kauli za ndani ya Sala zinatakiwa kutamkwa kiaai ya kua Mtu ni mwenye kuzisikia ndani ya Masikio yake kama ni mwenye kusikia.'** *(Rawdha Talibin)*

Na akasema tena Imam An Nawawi katika Al Majmuu kua: '**Kwa Maamuma basi hua ni Sunnah kwake kupunguza sauti, au Mtu anapokua anasali peke yake au katika Jamaa kiasi ya kua aweze kusikia Sauti yake na Masikio yake kama ni mtu asiekua na matatizo ya kusikia, na kama hana matatizo yanayompelekea kuzuilika kwa matamshi yake.**

Na hii inajumuisha Takbirat Ihram, Surat Al Fatiha, Tasbih, Tahiyyat, Salat Nabii, Salam n.k Yaani Kauli hio iwe ni Nguzo miongoni mwa Sunnah za Sala au ni Sunnah miongoni mwa Sunnah za Sala. **Kwani Kauli zote husika hua hazihesabiki hadi pale mtu husika atakapokua anakisikia kile anachokisoma.'***(Al Majmuu sharh Al Muhadhdhab)*

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Kama ikiwa Mtu husika ana matatizo ya Ulimi labda unamuuma kiasi ya kua hawezi kutamka, basi kwa mtu wa aina hii anatakiwa kuutikisa Ulimi wake kwa kadri atakavyoweza**. **Na akishafanya hivyo basi hatokua na haja ya kuirudia Sala yake, kwa sababu Sala yake itakua ni Kamilifu.'***(Al Majmuu)*

Na akasema Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Husein Ibn Ali Ibn Raslan Al Ramli Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Watu wenye Matatizo ya Ulimi au Ugumu wa Kusema basi huwabidi kuchezesha Ulimi wao kwa kadri wawezavyo pale wasemapo Takbirat Al Ihram, na kusoma Surat Al Fatiha, Tahiyyat n.**k.' *(GHashiyyah Al Bayan Sharh Zubad Li Ibn Raslan)*

NAMNA YA KUITEKELEZA SIJDAT SAHW

❖❖❖

Alhamd lillah tumeangalia kuhusiana na Nguzo za Sala kulingana na Mitizamo tofauti ya Wanazuoni na pia Tumeangalia kuhusiana na Sunnah Za Wajib na Sunna za Sunnah za Sala kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni tofauti.

Na tukasema kua Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam al Shafii basi Sijdat As Sahw Huhitajika kuletwa kutokana na Sababu Kuu 3 ambazo ni:

1-Az Ziyadah - Yaani kuongeza Kitendo miongoni mwa vitendo vya Ndani ya Sala.

2-An Naqs -Kupunguza Kitendo miongoni mwa vitendo vya ndani ya Sala.

Ash Shaq - Kua na Shaka kuhusiana na Utekelezwaji wa Kitendo husika ndani ya Sala.

Na tukafafanua juu ya yote haya Hivyo umefika wakati wa kukumbushana kuhusiana na namna ya Kutekeleza Sijda Sahw, huku tukikumbushana kua kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua Sijdat Sahw hua ni Sunnah Inayotiliwa Mkazo na Kupendekezwa na Wala si Wajibu

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi tunaona kua Inapendekezwa Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi ni kua Kama Mtu atakua amepunguza kitu ndani ya Sala yake basi Sijda Sahw hua ni Wajib, lakini kama ikiwa ameongeza kitu basi Sijda Sahw hua inapendekezwa.

Na Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na Baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi ni kua Sijdat Sahw ni Wajib kama ilivyoelezewa katika*(Fath Al Aalam Bi Sharh Al Murahid Al Anam)*

Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Sijda Sahw basi hua tunazungumzia Sijda ambayo ni yenye kua na Sifa stahiki sambamba kama Sijda za Ndani ya Sala, yaani Nguzo zake na Sunna zake ndio hizo hizo kwa kujumuisha Kugusisha Ardhi viungo Saba vya Mwili vya Kusujudia, yaani kugusisha Ardhini Paji la Uso pamoja na ncha ya Pua, Viganja vya Mikono yote miwili, Magoti yote Mawili na Vidole vya Miguu yote miwili huku vikiwa vimepinda na kuelekea Kibla.

Huku ndani yake ikiwemo kutobana mwili kwa Mwanamme yaani Kutoibanisha Mikono na Mbavu, Kutobamisha pamoja Magoti, kuyogusisha Mapaja na Tumbo.

Ambapo kwa upande wa Mwanammke basi hua ni kujikunyata kwa kadri atakavyoweza.

Ikiwemo pia mkao wa Iftirash baina ya Sijda mbili na mkao wa Tawarruk baada ya Sijda, na bila kusahau Dhikr zilizomo ndani yake. Na tunapozungumzia kuhusiana na Dhikr zilizomo ndani yake basi ingawa kuna Baadhi ya Wanazuoni Wanasema kua inatakiwa useme:

Subhanah Man la Yanam wala Yas-haw

Lakini kwa upande wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii basi yeye amesema kua: '**Mimi sikuona Chanzo cha Hadith chenye kuamrisha hivyo.'***(Talkhis Al Habir)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Muatawwali Al Shafii na Imam Al Adhrai Al Shafii basi wao wamenukuliwa wakisema kua: '**Dhikr Allah za Kwenye Sijdat As Sahw ndio zile zike Dhikr Allah zinazotumika kwenye Sijda ya ndani ya Sala**'*(Rawdha Talibin)*

Ama kuhusiana na Nia ya Sijda Sahw basi Wanazuoni wanasema kua Mtu inatakiwa uwe na nia hio ya kuleta Sijdat Sahw ndani ya Moyo wako pale unaposujudu lakini bila ya kuitamka. Na nia hio hua ni kwa Mtu anaesali peke yake, na Imam tu, kwani Maamuma hua hatakiwi kunuia kama alivyosema Imam Abd Allah Al Jurdani Al Shafii katika F*ath Al Allam.*

Kwa maana hio basi Ukiitamka nia hio basi Sala yako hubatilika kama asemavyo Imam Said Al Baishni Al Shafii katika *Bushra Al Karim.*

Imam Abu Al Ḥusayn 'Asakir Ad-Din Muslim Ibn Al Ḥajjāj Ibn Muslim Ibn Ward Al QushayriAnNaysābūrī, amenukuua Hadith tano tofauti zinazungumzia kuhusiana na Sijdat Sahw ambazo ni:

1-Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* inayothibitisha Sijdat Sahw lakini haikueleezea utekelezwaji wake, ambayo inasema kua:

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ يَحْيَى، قَالَ قَرَأْتُ عَلَى مَالِكٍ عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، عَنْ أَبِي سَلَمَةَ بْنِ عَبْدِ الرَّحْمَنِ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " إِنَّ أَحَدَكُمْ إِذَا قَامَ يُصَلِّي جَاءَهُ الشَّيْطَانُ فَلَبَسَ عَلَيْهِ حَتَّى لاَ يَدْرِي كَمْ صَلَّى فَإِذَا وَجَدَ ذَلِكَ أَحَدُكُمْ فَلْيَسْجُدْ سَجْدَتَيْنِ وَهُوَ جَالِسٌ "

Amesema Yahya Ibn Yahya kua : Nilisoma kwa Malik kutoka kwa Ibn Shihab, kutoka kwa Abu Salamah Ibn Abdul Rahman, kutoka kwa Abu Hurairah*Radhi Allahu Anhu*, kwamba. Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, "Anaposimama mmoja wenu kusali, Shaytani humjia na kumlchanganya kiasi kwamba hajui ni mara ngapi ameswali hivyo yeyote yule itakaemtokea hivyo basi na, asujudu sijda mbili akiwa amekaa."

2-Hadith ya Abu Buhaynah *Radhi Allahu Anhu* inayothibitisha Sijdat Sahw baada ya kukosekana Tahiyyat ya Mwanzo baada ya Rakaa ya pili, ambayo inasema kua Sijdat Sahw ililetewa baada ya Tahiyyat ya pili kabla ya Salam:

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ يَحْيَى، قَالَ قَرَأْتُ عَلَى مَالِكٍ عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ الأَعْرَجِ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ ابْنِ بُحَيْنَةَ، قَالَ صَلَّى لَنَا رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم رَكْعَتَيْنِ مِنْ بَعْضِ الصَّلَوَاتِ ثُمَّ قَامَ فَلَمْ يَجْلِسْ فَقَامَ النَّاسُ مَعَهُ فَلَمَّا قَضَى صَلاَتَهُ وَنَظَرْنَا تَسْلِيمَهُ كَبَّرَ فَسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ وَهُوَ جَالِسٌ قَبْلَ التَّسْلِيمِ ثُمَّ سَلَّمَ .

Amesema Yahya Ibn Yahya kua nilisoma kwa Malik kwa idhini ya Ibn Shihab, kwa idhini ya Abdul Rahman Al Araj, kutoka kwa Abdullah Ibn Buhaynah*Radhi Allahu Anhu*, alisema. *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, alitusalisha rakaa mbili katika sala ya Fardhi, kisha akasimama na hakukaa, watu wakasimama pamoja naye, hivyo alipomaliza sala na tulitegemea kua atatoa salamu. Akasema "Allahu Akbar" na akasujudu sijda mbili akiwa amekaa kabla ya salamu, kisha akatoa salamu.

3-Hadith ya Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* inayothibitisha Sijdat Sahw baada ya Mtu kua na Shaka ndaniya Sala yake, ambayo inasema kua Sijdat Sahw ililetewa baada ya Tahiyyat ya pili kabla ya Salam:

وَحَدَّثَنِي مُحَمَّدُ بْنُ أَحْمَدَ بْنِ أَبِي خَلَفٍ، حَدَّثَنَا مُوسَى بْنُ دَاوُدَ، حَدَّثَنَا سُلَيْمَانُ بْنُ بِلاَلٍ، عَنْ زَيْدِ بْنِ أَسْلَمَ، عَنْ عَطَاءِ بْنِ يَسَارٍ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " إِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ فِي صَلاَتِهِ فَلَمْ يَدْرِ كَمْ صَلَّى ثَلاَثًا أَمْ أَرْبَعًا فَلْيَطْرَحِ الشَّكَّ وَلْيَبْنِ عَلَى مَا اسْتَيْقَنَ ثُمَّ يَسْجُدُ سَجْدَتَيْنِ قَبْلَ أَنْ يُسَلِّمَ فَإِنْ كَانَ صَلَّى خَمْسًا شَفَعْنَ لَهُ صَلاَتَهُ وَإِنْ كَانَ صَلَّى إِتْمَامًا لأَرْبَعٍ كَانَتَا تَرْغِيمًا لِلشَّيْطَانِ "

Amesema Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Khalaf kua Musa bin Daud ametuhadithia, kua Suleiman bin Bilal ametuhadithia, kutoka kwa Zayd bin Aslam, kutoka kwa Ata Ibn Yasir, kutoka kwa Abu Said Al Khudri Radhi Allahu Anhu , ambaye amesema: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*,amesema: "Ikiwa mmoja wenu ana shaka na Salah yake na hajui ni mara ngapi amesali Rakaa Tatu au Nne" Basi Na aondoe shaka na atende yale aliyo yakini nayo, kisha asujudu sijda mbili kabla ya kutoa salamu, na ikiwa ataswali Rakaa tano basi zitaifanya Sala yake

iwe sawia kwa ajili yake, na kama ikiwa amesali Rakaa nne sawia basi itakua ni mwenye kumdhalilisha Shaytan.

4-Hadith ya Abd Allah Ibn Masud*Radhi Allahu Anhu* inayothibitisha Sijdat Sahw baada ya kuongezeka kwa kisimamo cha Rakaa ya 5, ambayo inasema kua Sijdat Sahw ililetewa baada ya Salam:

صَلَّى النبيُّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ: الظُّهْرَ خَمْسًا، فَقالوا: أزِيدَ في الصَّلَاةِ؟ قالَ: وما ذَاكَ قالوا: صَلَّيْتَ خَمْسًا، فَثَنَى رِجْلَيْهِ وسَجَدَ سَجْدَتَيْنِ.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* alisalisha Sala ya Adh Dhuhr kwa Rakaa Tano, Hivyo Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakauliza: 'Jee Sala imeongewa Kitu?' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema 'Kwanini?' Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Kwa Sababu Umetusalisha Rakaa 5' Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakunja Miguu yake na kisha akasjudu mara mbili.**

5-Hadith ya Dhu Al Yadayn*Radhi Allahu Anhu* inayothibitisha Sijdat Sahw baada ya baada ya Salat a Rakaa 4 kusaliwa kwa Rakaa mbili, ambayo inasema kua Sijdat Sahw ililetewa baada ya Tahiyyat ya pili kabla ya Salam:

عن أبي هُرَيرَة رَضِيَ اللهُ عَنْه، قال صلَّى بنا رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم إحْدَى صلاتَيِ العشيِّ – سمَّاها أبو هريرة، ولكن نسيتُ أنا– قال: فصلَّى بنا ركعتينِ، ثم سلَّمَ، فقام إلى :قال ابن سِيرين خشبةٍ معروضةٍ في المسجِدِ، فاتَّكأَ عليها كأنَّه غَضبانُ، ووضَعَ يَدَه اليُمنى على اليُسرى، وشبَّكَ بين أصابعِه، ووَضَع خَدَّه الأيمنَ على ظَهرِ كفِّه اليُسرى، وخرَجتِ السَّرَعانُ من أبوابِ المسجدِ، فقالوا: وعُمرُ، فهابَا أن يُكلِّماه، وفي القومِ رجلٌ في يديه طولٌ، يُقال قَصُرتِ الصَّلاةُ؟ وفي القومِ أبو بكرٍ له: ذو اليَدينِ، قال: يا رسولَ الله، أَنسيتَ أمْ قَصُرَتِ الصَّلاةُ؟ قال: لم أَنسَ ولم تَقصُر! فقال: أكَمَا يقولُ ذو اليدين؟ فقالوا: نعَمْ، فتقدَّم فصلَّى ما تَرَك، ثم سَلَّم، ثم كَبَّر وسجَدَ مِثلَ سُجودِه أو أطولَ، ثم رفَعَ رأسَه وكبَّر، ثم كبَّر وسَجَد مِثلَ سجودِه أو أطولَ، ثم رفَع رأسَه وكبَّر. فربَّما سألوه (أي: سألوا ابنَ سيرينثم سلَّم؟ فيقول: نُبِّئتُ أنَّ عِمران بن حُصَينٍ، قال: ثم سَلَّمَ

Amesema Muhammad Ibn Sirin kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha moja kati ya Sala za Jioni (Ambapo Imam Ibn Sirin anasema kua Abu Hurayrah Aliitaja Sala hio ila mimi nimeisahau) na akaihitimisha Sala hio baada ya Kuisalisha kwa Rakaa mbili tu. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka na kusimama kwenye karibu na Kigogo kilichopo mbele ya Msikiti na kuuweka mkono wake juu yake huku akiwa anaonekana kama kwamba amekasirika, akauweka mkono

wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto na kuvipitisha vidole vyake vya kulia baina ya vidole vyake vya kulia.

Ambapo Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* hawakuweza kusema chochote kutokana na kumuogopa na kumuheshimu *Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam*. Na wale Masahaba waliokua na Haraka wakaharakisha kutoka Nje, Huku wakiulizana kwa kusema: 'Vipi Leo Sala imefupishwa au?'

Hivyo Kuna Mtu aitwae Dhu Al Yadayn akamsogelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuuliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah Hivi Leo Sala Imefupishwa au umesahau?'

***Rasul Allah Sallallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La Haikufupishwa na wala Sikusahau.'**

Dhu Al Yadayn *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama haikufupishwa basi kwa hakika itakua Umesahau.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum:*'Hivi Jee Dhu Al Yadayn anasema kweli ama la?'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Naam, anasema Ukweli'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasimama. Na kusalisha Rakaa mbili zilizobakia ambazo alizisahau, na kisha akatoa Salam na akasema Allahu Akbar na kusjudu Sijdat ya Sahau ilizochukua mda wa kama Sijda za Kawaida au zaidi kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar na kisha Akasema Allahu Akbar na Kusujud tena Sijda ya pili na kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar.'

Ambapo Imam Muhammad Ibn Sirin alipoulizwa kuhusiana na kua 'Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam kumalizia ama la?'

Basi Imam Muhammad Ibn Sirin akasema kua: 'Mimi nimeambiwa na Imran Ibn Husayn *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam'*(Bukhari na Muslim)*

Hivyo kwa upande wa Imam Muhammad Idris Al Shafii basi yeye ana mitizamo mitatu kuhusiana na Sijdat Sahw ambayo ni:

1-Sijdat Sahw hua ni Kabla ya Kutoa Salam na baada ya Tahiyyat.

2-Kama Mtu akiongeza Kitu cha ziada ndani ya Sala basi ataleta Sijdat Sahw baada ya Kutoa Salam na kama ikiwa amepunguza basi ataleta Sijdat Sahw kabla ya Salam.

Ambapo Mtizamo wa Qawl Al Jadid hua ni Tofauti na mtizamo wa Al Qawl al Qadim yaani Mtizamo wa Zamani ambayo hua ni Mitizamo iliyotolewa katika Kitabu cha Al Risala kabla ya Imam Al Shafii kuhamia katika Ardhi ya Misri.

Na Mtizamo wa pili ni Mtizamo wa Al Qawl Al Qadim ambao ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik.

3-Mtu anaweza kuchagua kwa aidha kuleta Aijda Sahw kabla ya Salam ama baada ya Salam.

Ambapo Mtizamo wa kwanza ndio Mtizamo unaotegemewa zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii. Na Mtizamo huu wa Imam Al Shafii ni Mtizamo ambao alitumia katika Kutoa Fatwa alipohamia katika Ardhi ya Misri, na hivyo basi kujulikana kama Al Qawl Al Jadid yaani Mtizamo mpya wa katika kitabu chake cha Al Umm.Mtizamo wa Tatu pia ndio Mtizamo wa Imam Malik.

Kwani Fatwa ya Al Qawl Al Jadid ni yenye kutokana na Uthibitisho wa ile hadith isemayo kua:

صلى بهم الظهر فقام من الركعتين الأوليين ولم يجلس فقام الناس معه حتى إذا قضى الصلاة وانتظر الناس تسليمه كبر وهو جالس فسجد سجدتين قبل أن يسلم ثم سلم

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali katika Sala ya Adh Dhuhur pamoja na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum.*Ambapo alisimama kusali Rakaa mbili za mwanzo bila kukaa Tahiyyat, na Watu wakasimama pamoja nae. Na sala ilipomalizika basi Watu wakawa wanategemea kua kutakua na Salam, lakini badala yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema Allahu Akbar na kisha akasjudu Mara mbili na baada ya hapo akatoa Salam.(Sahih Bukhari)***

Ambapo katika sahih Muslim hadith hii ina maneno yasemayo:

ثم يسجد سجدتين قبل أن يسلم

Kisha akasjudu Sijda mbili kabla ya Salam.

Ambapo anasema Al Hafidh Imam Abu Umar Uthmani Ibn Abd Rahman Salahdin Al Qurdi Al Sharhazuri Al Shafii ambae ni maarufu kama Imam Ibn Salah kua; '**Kulingana na Hadith hii ambayo ni yenye Kupendelea *Qawl Al Adhhar* (Kauli ya Dhahir)kuhusiana na Suali hili la Sijda Sahw kua ni kabla ya Salaam basi hua ni Sahih, kutokana na Usahih wa Sanad ya Hadith hii na kua na Nguvu na Adhhar(Iliyokua wazi kabisa) kimaanaKwani Sababu ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuleta Sijda Sahw baada ya Kutoa Salam ni kutokana na kua aliisahau kabisa hadi alipokumbuka ilikua tayari ishapitiliza.'***(Badr Al Munir na Sharh Al Wasit)***

Ambapo anasema Imam Al Bayhaqi kua: '**Amesema Imam Az Zuhri kua:Mara ya mwisho *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuleta Sijdat As Sahw basi aliileta kabla ya Kutoa Salam.**' *(Sunan As Sughra Imam An Nasai)*

Na amesema Imam Al Zuhri kua;

انه آخر الأمرين من فعل رسول الله صلى الله عليه وسلم، ولأنه يفعل لإصلاح الصلاة، فكان قبل السلام كما لو نسي سجدة من الصلاة.

Kwani hili(La Sijdat Sahw) ni jambo la mwisho katika mambo mawili aliyoyafanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kwa sababu alilifanya kwa ajili ya kuiboresha Salah, hivyo kabla ya Taslim ilikuwa ni kama amesahau sijda ndani ya Sala.

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Mtizamo wa Al Jadid (Wa Imam Al Shafii) ni kua Sijdat Sahw sehemu yake hua ni baina ya Tahiyyat na Salam.'**

Hivyo Imam Al Ramli amesema kua: '**Maneno ya An Nawawi kua Sehemu yake, basi hua ni yenye kuashiria kua iwe mtu husika**. **Ameongeza kitu ama amepunguza ndani ya Sala yake basi Sijdat Sahw hua ni baina ya Tahiyyat na kile kinachofuatia baada ya Tahiyyat kisha Salat Ibrahimiyyah, na kisha Dua kisha ndio Sijdat Sahw kama alivyosali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kisha ndio Salam kiasi ya kua hakuna kinachotofautisha baina yake.'***(Nihayat Al Muhtaj)*

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua:'**Mtizamo wa Al Jadid (Wa Imam Al Shafii) ni kua Sijdat Sahw sehemu yake hua ni baina ya Tahiyyat na Salam**.'

Na Imam Ibn Hajar Al Haytami amesema kua:**'Maneno ya An Nawawi kua Sehemu yake, basi hua ni yenye kuashiria kua iwe mtu husika**, **Ameongeza kitu ama amepunguza ndani ya Sala yake basi Sijdat Sahw hua ni baina ya Tahiyyat na kile kinachofuatia baada ya Tahiyyat kisha Salat Ibrahimiyyah, na kisha Dua kisha ndio Sijdat Sahw kama alivyosali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kisha ndio Salam bila ya kutofautisha baina ya Sijdat Sahw na Salaam***(Tufah Al Muhtaj)**

Na akasema Imam Abd Allah Al Jurdani Al Shafii kua: '**Sijdat Al Sahw inatakiwa iletwe baada ya Tahiyyat na kinachofuatia baada yake yaani kama vile Salat An Nabii *Salallahu Alayhi wa Salam*, na Familia yake, na Dua**. **Lakini kama Mtu akiileta baada ya Tahiyyat na Salat An Nabii kabla ya kuisalia Familia ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.***

Basi hua hamna tatizo, na hii ni kwa sababu Sunnah yake hua imetekelezeka,na hua hairuhusiwi kuirudia Sijdat Sahw. **Hivyo hua ni Wajibu kuleta Sijda Sahw baada ya kumaliza Nguzo za Sala kabla ya Salam, ingawa Sijdat Sahw yenyewe hua ni yenye Kupendekezwa.Hivyo kama Mtu akiileta kabla ya kumaliza Nguzo za Ndani ya Sala(Kabla ya Nguzo ya Salam) basi Sala yake hua ni BatiliIsipokua pale itakapokua Mtu huyo ni *Maamuma Masbuq*(Maamuma aliechelewa) ambae humbidi kumfuata Imam hadi kwenye Sijda Sahw.**

Lakini kama Mtu akiwa hajachelewa basi akiileta Sijdat Sahw kabla kumaliza Nguzo za Ndani ya Sala basi Sala yake hubatilika kama alivyosema Imam Al Ramli. **Ambapo mtizamo wa Imam Ibn Hajar Al Haytami basi yeye anasema kua Katika Hali kama hii basi haibatiliki Sala ya Maamuma aliewahi wala aliechelewa'***(Bushra Al Karim)*

Naam..hivyo Imam Abd Allah Al Jurjani Al Shafii anaendelea kutuambia kua: '**Hua ni Wajibu kuleta Sijdat Sahw baada ya kumalizia Nguzo za ndani ya Sala yaani baada ya Tahiyyat na Salat An Nabii**, **Na hua haipendekezwi sana kuletwa baada ya Sunnah zilizopendekezwa.**

Kwa mfano baada ya Kuisalia Familia ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Dua inayofuatia baada yake. **Na pia kama Mtu akiileta kabla ya Kumaliza Nguzo za Ndani ya Sala basi Sala yake hubatilika**. **Isipokua kwa Maamuma Masbuq yaani Maamuma aliechelewa**
Hivyo Mtu akiwa hakuchelewa basi Sala yake hubatilika Na hii ni kulingana na mtizamo wa Imam Al Ramli. **Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Hajar Al Haytami basi hua haibatiliki***(Fat-h Al Allam)*

Ambapo Mwalimu wa Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Al Ghazali ambae ni Imam Abu Maali Al Haramain Sharfayn basi yeye ameelezea Njia tofauti ambazo zinazoelezea kukubalikakwa Sijdat Sahw

kama vile alivyoelezea Imam Al Shafii katika Kauli Tofauti, ambapo moja kati yao unaohesabika kua ni wa Al Qawl Al Qadim usemao kua Ukipunguza kitu ndani ya Sala basi Sijdat Sahw baada ya Salam ya kwanza na kama ukizidiaha basi Kabla ya Salam ndio anaoufuata Imam Malik.

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi anasema kuaMtizamo wa Al Qawl Al Qadim unaofuatwa na Imam Malik ni wenye Nguvu zaid na kisha ndio unafuata Mtizamo wa Al Qawl Al Jadid. Na mbali ya Kua Al Qawl Al Qadim una Nguvu lakini Mtizamo Unaokubalika zaid kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni kua: '**Sijdat Sahw huletwa kabla ya Kutoa Salam na Mara tu baada ya Tahiyyat ya mwisho**. **Yaani baada ya Kumsalia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,na familia yake na kuomba Dua ya baada ya Tahiyyat basi ndio unaleta Sijda mbili kisha Unatoa Salam za kuashiria kumalizia Sala yako.**'

Na Kwa kua Mtu unakua ni mwenye kujua Kua Umekosea basi hua inatakiwa kunuia Ndani ya Moyo wako kua, Unaleta Sijda Sahw kwa Kafidia Kasoro iliyojitokeza ndani ya Ibada yako ya Sala.

Ama tunapoangalia kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi Wanazuoni wao wa Fiqh wanasema kua:**'Sijdat Sahw hua inaletwa baada ya Salam ya Kwanza, ambapo baada yake mtu hua unatakiwa kusoma Tahiyyat yena upya.'**

وَإِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ فِي صَلَاتِهِ فَلْيَتَحَرَّ الصَّوَابَ فَلْيُتِمَّ عَلَيْهِ ثُمَّ لِيُسَلِّمْ ثُمَّ يَسْجُدُ سَجْدَتَيْنِ

Na hii ni kutokana na Hadith isemayo kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

'Kama ikiwa mmoja miongoni mwenu amekua na Shaka ndani ya Sala yake basi na akisie na kisha amalize Sala yake. **Kisha atoe Salam na kisha asujudu Sijda mbil**i'*(Sahih Bukhari)*

Na anasema Imam Abd Allah Ibn Mahmud Al Mawsul Al Hanafi katika Kitab Al Ikhtiyar kua: '**Mtu anapoleta Sijdat Sahw basi hua anayakiwa asujudu Mara mbili baada ya Kuto Salam na kisha Anasoma Atahiyyat na Kutoa Salam**. **Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua:**

لِكُلِّ سَهْوٍ سَجْدَتَانِ بَعْدَ السَّلَام

Kwa Kila Kusahau ndani ya Sala basi hua ni Sujud mbili baada ya Sala.

Na pia imenukuliwa na Imran Husein na Masahaba kadhaa *Radhi Allahu Anhum* kua:

أَنَّهُ – صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ – سَجَدَ سَجْدَتَيِ السَّهْوِ بَعْدَ السَّلَامِ

'Hakika yeye *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisujudu Sijdah mbili baada ya Salam.

Na imenukuliwa kua alikua akitoa Salam mbili na pia imenukuliwa alikua akitoa salam moja,na huo ndio Mtizamo sahih zaid. **Kwani Husema Allahu Akbar kisha husujudu na kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa Tasbih na kisha hunyanyua Kichwa na kisha husjudu tena,na kisha husoma Tahiyyat na kuomba Dua kwa sababu sehemu ya kuomba Dua katika Sala hua ni Mwishoni mwa Sala husika.'**

Na amesema Imam Ala Ad Din Abu Bakr Ibn Masud Al Kasani Al Hanafi kua: '**Ama kulingana na Madhhab yetu ya Hanafi basi hua inapendekezwa kuleta Sijdat Sahw baada ya Salam**. **Iwe mwenye kufanya Ibada amepunguza kitu au amezidisha kitu ndani ya Sala kitakachomhitajia kuleta Sijdat Sahw.**

Hivyo Mtu huyu baada ya kumaliza Sala yake kwa Tahiyyat basi atatoa Salam, kisha atasema Allahu Akbar Na kisha atalea Sijda mbili za Sahw na kisha atanyanyua kichwa chake huku akisoma Takbir na kisha atasoma Tahiyyat na kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kuomba Dua zake,na kisha atatoa Salam.

Na huu ndio Mtizamo wa Imam Al Kharki na pia wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Hanafi, Lakini hata hivyo pia hua inakubalika Kuleta Sijdat Sahw Kabla ya Kutoa Salam, yaani kama Mtu ataleta Sijda Sahw kabla ya Kutoa Salam, basi hua haina haja kwake kuirudia Sala yake kwa sababu hua tayari ameshakamilisha Nguzo za Sala yake.

Na ingawa itakua amefanya hivyo inavyokubalika pia lakini atakua ni mwenye kudharau mpagilio unaotakiwa wa kuleta Sijdat Sahw ambao hua ni baada ya Kutoa Salam.' *(Badai Al Sanai -Imam Al Kasani)*

Kwani anasema pia Imam Uthman Ibn Ali Al Zaylai Al Hanafi kua; '**Mtizamo wa Tatu kuhusiana na ni niji iinachotakiwa kufanywa baada ya Kuleta Sijda Sahw ni kama ilivyoelezewa kua ni Kuaoma Tahiyyat na Taslim baada ya Kuleta Sijdat Sahw. Na hii ni kutokana na uthibitisho wa Hadith iliyonukuliwa na Imam Abu Daud isemayo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*alifanya Sijda mbili za Sahau na kisha akasoma Tahiyyat na kisha akatoa Salam.**

Na Wanazuoni wana mitizamo tofauti kuhusiana na namna ya Kutoa Salam, kwani kuna wasemao kua Mtu anaesali hua anatakiwa kutoa Salam mbili kulia na kushoto. **Ambapo huu ndio Mtizamo unaoonekana kua ndio Sahih zaidi,na hii ni kutokana na Mfano wa Hadith ya Imam Abu Daud ambayo inaashiria kua Salam hio ilikua ni Salam ya kawaida.**

Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa Shams Aimah Fakhr Al Islam (Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Abi Sahl Al Sarkhasi Al Hanafi) ambae amesema kua: '**Taslim (Kutoa Salam) Moja kuelekea Upande wa Kibla hutosheleza kwa sababu Taslim hua inakusudiwa kua ni Salam zaid kuliko kua Mwisho wa Sala.'**

Napia kuna Wanazuoni wasemao kua Mtu hua anatakiwa atoe Salam katika Upande wa Kulia tu.Kwani Imam Khawahir Zaddah amesema kua: 'Mtu anaesali hua hatakiwi Kuleta Sijda Sahw baada ya **Sijda mbili na hii ni kwa sababu Sijda Sahw hii hua itahesabiwa kua ni nje ya Sala.'Ambapo Mtu anaesali anatakiwa Amsalie *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na kisha asome Dua za mwisho wa Sala, baada ya Kuleta Sijda Sahw. Na huu ndio Mtizamo Sahih zaidi kutokana na kua mambo haya hua yanafanywa mwishoni mwa Sala, Ambao huu ndio Mtizamo wa Imam Al Kharki.**

Na imesemwa pia kua Mti anatakiwa Amsalie Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam Na kisha asome Dua Stahiki katika Tahiyyat ya mwanzo ya kabla ya Taslim, lakini Imam Tahtawi amesisitiza kua Katika kila Kikao cha Tahiyyat kinachomalizikia na Taslim hua mnatakiwa Kusaliwa kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani yake. Na kutokana na Mtizamo huu basi Mtu mwenye Kusali hua anatakiwa amsalie *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat zote.

Ila, Wanazuoni wa awali kama Imam Abu Hanifa na Imam Abu Yusuf basi wao wametofautiana na Mtizamo huu,kwani wao wanasema kua: 'Mtu hua anatakiwa Kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Tahiyyat ya kwanza kabla ya Taslim.'

Na kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Hasan basi yeye anasema kua Mtu hua anatakiwa amsalie *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika kikao cha pili cha Tahiyyat baada ya Sijdat Sahw. Ingawa Imam Abu Hanifa na Imam Abu Yusuf wao wanaamini kua Taslim hua ndio inayofunga Sala Na hivyo wanaamini kua kikao cha kwanza cha Tahiyyat kabla ya Sijdat Sahw, ndio kinachomalizia Sala, na hivyo ndani yake ndio Mtu anatakiwa amsalie R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na kuomba Dua stahiki ili amalizie Sala yake kulingana na mpangilio wa Nguzo za Sala, wa Sunna na yanayopendekezwa ndani ya Sala.Na imesemwa katika Al Mufiid kua hii ndio njia Sahih

Tunapoangalia kwa Upande wa Imam Muhammad Ibn Hasan basi yeye ana mtizamo wa kua: 'Kikao cha kabla ya Sijdat Sahw sio kikao kianchohitimisha Sala, na hivyo Mtu anatakiwa amsalie *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha asome Dua Stahiki katika kikao cha pili baada ya Sijdat Sahw, kwani hicho ndio kikao kinachohitmishia Sala'*(Tabiyn Al Haqaiq Sharh Kanz Daqaiq)*

Hivyo bila ya shaka tunapoangalia Ufafanuzi wa Imam Al Zaylai kuhusiana na Sijda Sahw kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, basi tunaona kua: '**Mtizamo wa Maimamu wawili wakuu wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambao ni Imam Abu Hanifa na Imam Abu Yusuf Ndio Mtizamo ambao Unaenda Sambamba na Mtizamo wa Imam Malik na pia unendana Sambamba na Mtizamo Unaoaminika na kukubalika wa Madhhab ya Imam Al Shafii**. **Ambao ni kua Sijdat Sahw inaletwa kabla ya Taslim yaani baada ya Kumalizika Tahiyyat ya Mwisho na Salat An Nabii na Kumalizika kwa Dua Stahiki, basi unasjudu Mara mbili kisha unatoa Salam**

Ama kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ambapo tunaona kua wao wanasema kua:**'Hua ni Wajib kusoma Tahiyyat baada ya Sijda Sahw ambayo hua inaletwa baada ya Salam.'**

Na haya yanathibitishwa na Imam Ibrahim Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Muflih Al Maqdisi Al Hanbal pale aliposema katika kitabu chake cha Al Mubdi Sharh Al Muqni ambacho ni kitabu kilichoweka Historia katika Fiqh ya Madhhab ya Hanbal kua: '**Mtu anaposujudu Sijdat Sahw baada ya Taslim, iwe kutokana na kukusudia kuileta Sijda Sahw hio baada ya Taslim ama kabla ya Taslim na hivyo akasahau na kuileta baada ya Taslim**. **Basi anatakiwa asome tena Tahiyyat ya Mwisho upya ambapo huu hua ni Wajibu**. **Na huu ndio Mtizamo pia wa Kundi la Wanazuoni akiwemo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* Ahmad Ibn Hanbal ambapo tunaona kua wao wanasema kua:**'**Hua ni Wajib kusoma Tahiyyat baada ya Sijda Sahw ambayo hua inaletwa baada ya Salam.'**

Kutokana na Uthibitisho wa Hadith ya Imran ambae amesema kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisahau kitu katika Sala, hivyo akaleta Sijda Sahw mbili na kisha akasoma Tahiyyat na kisha akatoa Salam.'*(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhii)***

Ambapo kwa upande wa Imam At Tirmidhii basi yeye amesema kuhusiana na Hadith hii kua ni HasanHadithHivyo Mtu anatakiwa asome Tahiyyat baada ya Sijda Sahw kwa sababu Sijdat Sahw hua ni Sujud inayohitajia kua na Taslim. Na kwa kua inahitajiwa kua na Taslim basi inabidi ifuatiwe na Tahiyyat kabka yake, na kisha ndio ije Taslim, kama vile ilivyo katika Sala ya Kawaida, katika Tahiyyat ya mwisho ya Sala, ambapo Mtizamo mwengine pia ni kua Haitakiwi

kwa Mtu kusoma Tahiyyat baada ya Sijdat Sahw, yaani inatosha Kutoa Salam baada ya Sijda Sahw, ambapo huu ni Mtizamo wa Taqi Ad Din Ibn Taymiyyah.'*(Sharh Al Muqni)*

Na amesema pia Imam Al Buhuti Al Hanbali kua: '**Wakati Mtu anapoleta Sijda Sahw baada ya Taslim basi anasoma Tahiyyat ya Mwisjo na kisha Anatoa Salam, iwe sehemu stahiki ya Sijdat Sahw baada ya Taslim au baada ya Taslim.'***(Daqaiq Uuli Nuuha Sharh Muntaha Al Iraadat)*

Na kwa upande wa Imam Abd Rahman Al Bali Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Wakati Mtu anaesali anapofanya Sijdat Sahw kabla ya kutoa Salam, basi hua na wajibu wa kuifanya Sijda Sahw hio baada ya Tahiyyat ya mwisho na kisha ndio anatakiwa Atoe Salam.'** *(Rawdha An Nadhir Sharh Kaafi Al Mubtadi)*

Kwani baada ya kuangalia Mitizamo tofauti kuhusiana na Sijdat Sahw na namna ya Kuileta kwake basi tunaona kua:

'Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii Sijdat Sahw hua si Wajib bali hua ni Sunna inayopendekezwa kama alivyosema Imam An Nawawi katika *Rawdah Talibin.*

Ambapo pia kuna Mtizamo mmoja katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa unaoungana mkono na mtizamo huu wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Sijdat Sahw ni yenye kupendekezwa.

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi tunaona kua wao wanasema kua Sijda Sahw hua ni Wajib.

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: 'Kama ikiwa Mtu ameacha Kitu ndani ya Sala yaani hakukitekeleza basi hua ni Wajib kuleta Sijdat Sahw, na kama akiongeza basi kitu basi Sijdat Sahw hua ni yenye kupendekezwa kama ilivyoelezwa katika *Fat-Al Alam bi Sharh Murahid Al Anam.'*

Imam Muslim anasema katika Sahih Muslim kua:

وَحَدَّثَنِي مُحَمَّدُ بْنُ أَحْمَدَ بْنِ أَبِي خَلَفٍ حَدَّثَنَا مُوسَى بْنُ دَاوُدَ حَدَّثَنَا سُلَيْمَانُ بْنُ بِلاَلٍ عَنْ زَيْدِ بْنِ أَسْلَمَ عَنْ عَطَاءِ بْنِ يَسَارٍ عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ قَالَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ إِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ فِي صَلاَتِهِ فَلَمْ يَدْرِ كَمْ صَلَّى ثَلاَثًا أَمْ أَرْبَعًا فَلْيَطْرَحِ الشَّكَّ وَلْيَبْنِ عَلَى مَا اسْتَيْقَنَ ثُمَّ يَسْجُدُ سَجْدَتَيْنِ قَبْلَ أَنْ يُسَلِّمَ فَإِنْ كَانَ صَلَّى خَمْسًا شَفَعْنَ لَهُ صَلاَتَهُ وَإِنْ كَانَ صَلَّى إِتْمَامًا لأَرْبَعٍ كَانَتَا تَرْغِيمًا لِلشَّيْطَانِ

Na Amesema Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Khalafi kua amesema Musa Ibn Daud kua amesema Sulayman Ibn Bilal kua amesemaZayd Ibn Aslam kua amesema Ataa Ibn Yasir kuamesema Abu Said Al Khidhr *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Kama ikimjia shaka yeyote yule miongoni mwenu ndani ya Sala, na ikawa hamna uhakika umeshasali Rakaa ngapi, yaani kama ni Rakaa Tatu au Nne basi n aachane na shaka hio na kusimamia Sala yake kutokana na Msingi wa Idadi aliyokua na uhakika nayo. Na kisha asujudu mara mbili kabla ya kutoa Salam kama kwamba amesali Rakaa Tano, hivyo Sala yake itakua imeingilia kati kwa ajili yake. Na akam ikiwa amesali Rakaa Nne, basi Sijda itamkera Shaytani.' *(Sahih Muslim)*

Hivyo Sijdat Sahw imewekwa kwa Ajili ya Kufidia Kitu kilichosahauliwa ndani ya Sala, na pia kwa lengo la Kumkera Shaytan ambae ni mwenye kumghafilisha Mtu ndani ya Sala yake. Na hivyo pia Sijdat Sahw kua na lengo la Kumfurahisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* kutokana na Mja husika kurudi kwa Mola wake kwa ajili ya kurekebisha makosa yake.

Kama anavyoelezea Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi pale aliposema kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Sujud Mbili za Sahw hua ni zenye kumkasirisha Shaytan.'***(Sahih Muslim)*

Yaani Mtu anapoleta Sijdat Sahw basi Ibilisi hukasirika kutokana na Kudhalilika, ambapo hadith imetumia neno *Targhim* lenye kutokana na neno *Al Ragham* lenye kumaanusha Udongo.

Neno hili hua linatumika katika maneno ya Dua yasemayo kua: *Arghama Allahu Anfuhu* yaani Allah amdhalilishe mtu husika.

Yaani maana yake ni kua kutokana na kua Shaytan ndie anaemghafilisha Mtu husika. **Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amejaalia njia kwa Mja wake huyo kurekebisha Sala yake, kulipa Fidya kwa Mghafiliko uliosababishwa na Shaytan dhidi yake na pia kushikamana na amrisho la *Allah Subhanah wa Ta'al*a ambalo Shaytan aligoma kulitekeleza pale alipoamrishwa asujudu, wa Allahu Aalam.'** *(Al Minhaj -Imam An Nawawi)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Buhuti Al Hanbali basi yeye amesema kua: '**Sijda imeamrishwa kufanywa mara mbili katika kila Rakaa ya Sala**. **Ambapo hii hua ni tofauti na vitendo vyote vya Sala, na hii ni kwa sababu hali ya Kusujdu hua ni yenye kumpelekea Ibn Adam kua katika hali ya Juu kabisa ya Unyenyekevu.**

Kwani baada ya kua ni mwenye kusimama na kurukuu basi hua ni mwenye kuifikia Darja hio ya Juu ya Unyenyekevu kwa Kumsujudia Mola wake. **Na kutokana na kuifikia Darja hio basi hua ni mwenye kutakiwa kukaa kitako kwa ajili ya kumtumikia Mola wake**. **Na hivyo Mtu husika hupata nafasi nyengine ya Kusujudu kwa ajili ya kuonesha Shukran.**

Kutokana na kua ni mwenye kufadhiliwa kwa kuchaguliwa kua ni mwenye Kumtumikia Mola wake katika Ibada. **Na hivyo kua ni mwenye kuepushwa na kuokolewa kutokana na vishawishi vya Ibilisi, na kua ni mwenye kuongozwa na Mola wake katika Kumuabudu kutokana na wingi wa Rehma zake juu yake.'**

Kwani anasema Mujtahid Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii ambae ni Mwanafunzi wa Imam Al Rabbi Ibn Sulayman ambae ni mwanafunzi wa Mujtahid Imam Muhammad Idris Al Shafii kua:

'Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Utekelezwaji wa Sijda Sahw kwa Mitizamo 6 ambayo ni kama ifuatavyo:

1-Kuna wenye Mtizamo wa kua Hua hakuna kisomo cha Tahiyyat wala Salat An Nabii ndani yake baada yake ambapo huu ni Mtizamo wa Anas Ibn Malik Radhi Allahu Anhu, Imam Hasan Al Basr na Imam Ataa.

2-Kuna wenye Mtizamo wa kua Baada ya Sijdat Sahw basi kuna kisomo cha Tahiyyat na Salat An Nabii.

3-Kuna wenye Mtizamo wa kua Baada ya Sijdat SahwBasi Mtu anatakiwa asome Tahiyyat tu bila kumsalia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Al Hakam, Imam Hamad Ibn Salamah na Imam Ibrahima An Nakhai.

4-Kuna Mtizamo wa kua baada ya Sijda Sahw basi haitakiwi kusoma Tahiyyat, bali inatakiwa Salat An Nabii tu. Ambapo huu ni mtizamo wa Imam Muhammad Ibn Sirrin.

5-Kuna wenye Mtizamo wa kua baada ya Sijdat As Sahw basi kama Mtu anaweza kusoma Tahiyyat na Salat An Nabii kama anataka, na kama hataki basi haina haja, ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Ataa.

6-Kuna wenye Mtizamo ambao ni wa Imam Ahmad Ibn Hanbal usemao kua kama mtu akileta Sijda sahw kabla ya Salam basi hasomi Tahiyyat. Na akiileta baada ya Salam basi atasoma Tahiyyat.'

Kisha Mujtahid Imam Abu Bakar Al Mundhiri Al Nishapuri anaendelea kutuambia kua: '**Ukweli ni kua imethibitishwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* alipoleta Sijdat Sahw basi alisujudu mara 4 ndani yake, na pia alitoa Salam baada yake. Lakini kuhusiana ushahidi wa Kisomo cha Tahiyyat baada yake basi kuna Shaka ndani ya vithibitisho vyake**. *'(Bidayat Al Mujtahid, Al Ishraf)*

Na akasema tena Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua: '**Sifikirii kua Kisomo cha Tahiyyat baada ya Sijdat Sahw kua kimethibitishwa.'**

Hivyo basi kwa maana hio tunaona kua Ingawa kuna hadith kuhusiana na Tahiyyat baada ya Sijdat Sahw kutoka kwa Abd Allah Ibn Masud R*adhi Allahu Anhu* kama alivyonukuu Imam Abu Daud na Imam An Nasai.

Na pia kuna hadith kuhusiana na Tahiyyat baada ya Sijda Sahw kutoka kwa Al Mughira *Radhi Allahu Anhu* kama alivyonukuu Imam Al Bayhaqi.

Lakini hata hivyo kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii akiwemo na Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri basi tunaona kua Hadith 3 hizi ni dhaifu, na ndio maana hazikufanyiwa kazi.

HUKMU YA SIJDAT SAHW

❖❖❖

Naam..tumeingia kwenye Sehemu ambayo inawaumiza sana vichwa watu ambayo ni kuhusiana na Hukmu za Sijdat Sahw.Na bila ya shaka hii ni sehemu ya Maada ambayo ni ndefu kidogo na inachanganya, hivyo naomba utulivu wa ufaham wa kila mwenye kutaka kufaham juu yake Mada hii.

Ambapo kabla ya kuendelea basi kwanza tunakumbushana kua:**'Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii Sijdat Sahw hua si Wajib bali hua ni Sunna inayopendekezwa kama alivyosema Imam An Nawawi katika *Rawdah Talibin.'***

Ambapo pia kuna Mtizamo mmoja katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa unaoungana mkono na mtizamo huu wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Sijdat Sahw ni yenye kupendekezwa.

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi tunaona kua wao wanasema kua Sijda Sahw hua ni Wajib.

Na kwa upande wa Wanzuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: 'Kama ikiwa Mtu amefuta Kitu ndani ya Sala yaani hakukitekeleza basi hua ni Wajib kuleta Sijdat Sahw, na kama akiongeza basi kitu basi Sijdat Sahw hua ni yenye kupendekezwa kama ilivyoelezwa katika *Fat-Al Alam bi Sharh Murahid Al Anam.'*

Kwani tumeyarudia haya kwa sababu Ndio Msingi wa Kila tutakachokielezea ndani ya Mada hii ya Hukmu za Sijda Sahw.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii Sijdat Sahw hua si Wajib bali hua ni Sunna inayopendekezwa kama alivyosema Imam An Nawawi katika *Rawdah Talibin*na ingawa Sijdat Sahw hua ni Sunnah lakini Sijdat Sahw hua pia ni Fardhi lakini katika hali moja tu, ambayou ni pale Mtu anapokua ni Maamuma kisha Imam wake akaleta Sijdat Sahw basi kwa Maamuma husika Sijdat Sahaw hii hua ni Fardhi kwake, kwa sababu ni lazima kwake kumfuata Imam wake katika Sala Husika.

Na Amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yhaya Ibn Sharaf An-Nawawi kua: 'Kama Imam ataleta Sijda Sahw moja tu, basi Maamuma atatakiwa alete Sijdat Sahw ya pili kwani hua ni mwenye kutakiwa kuchukulia kua Imam amekosea. Na kama ikiwa Imam amefanya kwa makusudikutoleta Sijdat Sahw, au kwa kukosea basi yule aliekua nyuma yake hua n Wajibu wa kuileta Sijdat Sahw hio. Na huu ndi Mtzamo uliotajwa na Wanazuoni, kwa sababu wakati Imam anapokosea hua ni mwenye kusababisha Sala za Maamuma wake kua n zenye kasoro pia, kwa sababu ya kukosea kwake hivyo kama Imam hakufidia kasoro hio basi wale walioko nyuma yake hua wanatakiwa wafidie kasoro hio k wenye Sala zao kwa kuleta Sijdat Sahw' *(Al Majmu' (4/65)*

Na kama Imam akikosema katika Sala nakisha akawa hakuleta Sijdat Sahw basi Mtizamo sahihi wa Madhhab yetu ni kama tulivyosema hapo kabla kua wale wanaosali nyuma yake wanatakiwa walete Sijdat Sahw. Na huuu ndio pia mtizamo wa Malik, Al Awzai, Al Layth na Abu Thawr ambao umenukuliwa kutoka kwa Ahmad, Ibn Al mundhir, Ibn Sirin, Al Hakam, Qatadah, Ata, Al hasan, An Nakhai, Al Qasim, Hammad Ibn Sulayman, Ath Tawry Abu Hanifa Al Muzani na pia kuna Mtizamo kuoka kwa Ahmad usemao kua: Maamuma hua hatakiwi kuleta Sijdat Sahw inapotokea halai kama hii.'*(Al Majmu)***

Ambapo pia kuna Mtizamo mmoja katika Madhhab ya Imam Abu Hanifa unaoungana mkono na mtizamo huu wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Sijdat Sahw ni yenye kupendekezwa.

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi tunaona kua wao wanasema kua Sijda Sahw hua ni WajibNa hii ni kwa sababu Wanazuoni wameyofautiana kuhusiana na Jibu la Suali lisemalo: **'Jee kwa Mtu ambae amesahau Kitu ndani ya Sala na hivyo akaongeza au akapunguza kitu ndani ya Sala yake na kisha akasahau kuleta Sijdat Sahw ndani ya Sala yake, Afanyeje?'**

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua:**'Mtu aliesahau ndani ya Sala na kisha akasahau kuleta Sijda Sahw baada yake basi anatakiwa pale pale baada ya Sala anapokumbuka wakati hajaondoka kutoka kwenye Msala wake au sehemu aliyosalia au Msikitini, basi ni kuleta Sijda Sahw hio.'**

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua:**‘Mtu aliesahau ndani ya Sala na kisha akasahau kuleta Sijda Sahw baada yake basi anatakiwa**kabla hajaondoka Katika sehemu aliuosalia Atofautishe baina ya kua jee Sijda hio inatakiwa kabla au baada ya Salam, Na kisha baada ya hapo anatakiwa Asujudu kama ni Sijda ya Kabla ya Salam, Lakini kama itakua ni Sijda ya baada ya Salam basi atatakiwa asujudu hata kama ikiwa amekumbuka baada ya Masiku kupita.’

Ambapo kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua: ‘**Mtu aliesahau ndani ya Sala na kisha akasahau kuleta Sijda Sahw baada yake basi hua hamna tatizo na Sala yake Mtu inakua Sahih.’**

Na hii ni kwa sababu kutokana na kua Sijdat Sahw ni Sunnah ambayo sehemu yake hua ni kabla ya Salam, hivyo kama mtu akitoa Salam kwa makusudi huku akijua kua amesahau kitu, na ukapita mda basi sehemu yake Sijdat sahw hua imeshakosekana, lakini kama si mda mrefu basi anaweza akaileta au akaiwacha.

Ambapo kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: ‘**Mtu aliesahau ndani ya Sala na kisha akasahau kuleta Sijda Sahw baada yake basi kama itakua haujapita Mda mrefu basi itabidi Alete Sijdat Sahw na kama umeshapita Mda au Udhu umeshamtoka basi hua haina haja kuleta Sijdat Sahw na Sala yake ni Sahih.’**

Kwani inasema *Al Mawsuah Fiqhiyyat Kuwatiyah* kuhusiana na Kusahau Sijda Sahw baada ya Kusahau Ndani ya Sala kua: ‘**Kama ikiwa Muumini amesahau Kuleta Sijdat Sahw baada ya kusahau kwake ndani ya Sala, na kisha akamaliza Sala bila ya Kusujudu basi juu yake kuna Maelezo yafuatayo:’**

Kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua, Mtu husika hua hatakiwi Kusujudu Sijda Sahw kama ikiwa hakukusudia Kusujudu, na hivyo kua ni mwenye kutoa Salam yenye lengo la Kuifunga Sala na kutoka Nje ya Sala huku akiwa ni mwenye kugeukia Upande ambao sio wa Kibla, au akiwa anazungumza au akiwa anaondoka Msikitini.’

Ama kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua:Kuna tofauti baina ya Mtu kukuleya Sijda sahaw kabla au baada ya Salam. Kwani akiisahau Sijda Sahw ya Baada ya Salam, basi hua anatakiwa ailete Sijda hio pale atakapokumbuka hata kama ikiwa ni baada ya mwaka.

Kwani Sijda Sahw ya Baada ya Salam hua haifutiki iwe imeachwa kwa Makusudi au kwa kusahau, kwa Sababu Lengo la Sijdat Sahw ni Kumdhalilisha Shaytan kama ilivyosemwa Kwenye Hadith, Ama kuhusiana na Sijda Sahw ya kabla ya Salam basi Mipaka yake hua ni pale mtu atakapokua ameshaondoka katika sehemu aliyosalia. Hivyo kama mtu ameshaondoka Maikitini na ameahafika kwake, au ameshafika mbali na mda Mrefu umeshapita, basi hua haina haja kuileta.

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Basi wao Wanasema kua: Kama ikiwa Mtu amesahau kuleta Sijdat Sahw kutokan na kusahau kwake ndani ya Sala,na kisha akatoa Salam kwa kukosea au kwa kusahau au akakumbuka baada ya mda kupita basi hua haina haja kwake kuileta Sijdat Sahw hio.

Na hii ni kwa Sababu Wakati na Sehemu ya Kuleta Sijda Sahw ndani ya Sala hua Imeshakosekana kutokana na kutolewa Salam inayomtoa Mtu nje ya Sala Jambo ambalo hua haliwezekani kurekebishwa kutokana na tukio hilo la Salam. Ama kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: Kama ikiwa Mtu atasahau Kuleta Sijdat

Sahw kutokana na kusahau kwake ndani ya Sala, iwe kabla au baada ya Sala, basi Mtu husika hua anatakiwa Kuileta Sijdat Sahw hio hata kama ikiwa ameshazungumza maneno mengine wakati yupo katika sehemu aliyosalia Isipokua, kama ikiwa umeshapita Mda mrefu, au ameshatokwa na Udhu, au ameshaondoka katika sehemu aliyosalia.'*(Mawsuah Fiqhiyyah Quwaytiyyah)*

Naam..tunapoangalia Mitizamo ya Hukmu hii, basi tunaona kua msingi wake ni wa ile hadith ya Dhu Al Yadayn ambayo *Rasul Allah Salllahu Alayhi wa Salam* alisalisha Salat Dhuhr kwa Rakaa mbili kisha akatoa Salam.

Na hii ni kama tulivyoona katika Mfano wa Hadith Ya Dhul Yadayn ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisalisha Sala ya Al Asr na kutoa Salam badala ya Rakaa 2 ambayo inasema: '**Abd Allah Ibn Yusuf kua amesema Malik Ibn Anas kua amesema Ayoub Al Sakhtiyani kua:**

عن أبي هُرَيرَة رَضِيَ اللهُ عَنْه، قال صلَّى بنا رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم إحْدَى صلاتَيِ العشيِّ – سمَّاها أبو هريرة، ولكن نسيتُ أنا– قال: فصلَّى بنا ركعتينِ، ثم سلَّمَ، فقام إلى :قال ابن سِيرين خشبةٍ معروضةٍ في المسجِدِ، فاتَّكأَ عليها كأنَّه غَضبانُ، ووضَعَ يَدَه اليُمنى على اليُسرى، وشبَّكَ بين أصابعِه، ووَضَع خَدَّه الأيمنَ على ظَهرِ كفِّه اليُسرى، وخرَجتِ السَّرَعانُ من أبوابِ المسجدِ، فقالوا: وعُمرُ، فهابَا أن يُكلِّماه، وفي القومِ رجلٌ في يديه طولٌ، يُقال قَصُرتِ الصَّلاةُ؟ وفي القومِ أبو بكرٍ له: ذو اليَدينِ، قال: يا رسولَ الله، أَنسيتَ أمْ قَصُرَتِ الصَّلاةُ؟ قال: لم أَنسَ ولم تَقصُر! فقال: أكَمَا يقولُ ذو اليدين؟ فقالوا: نعَمْ، فتقدَّم فصلَّى ما تَرَك، ثم سَلَّم، ثم كَبَّر وسجَدَ مِثلَ سُجودِه أو أطولَ، ثم رفَعَ رأسَه وكبَّر، ثم كبَّر وسَجَد مِثلَ سجودِه أو أطولَ، ثم رفَع رأسَه وكبَّر. فربَّما سألوه (أي: سألوا ابنَ سيرينثم سلَّم؟ فيقول: نُبِّئتُ أنَّ عِمران بن حُصَينٍ، قال: ثم سَلَّمَ

Amesema Muhammad Ibn Sirin kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha moja kati ya Sala za Jioni (Ambapo Imam Ibn Sirin anasema kua Abu Hurayrah Aliitaja Sala hio ila mimi nimeisahau) na akaihitimisha Sala hio baada ya Kuisalisha kwa Rakaa mbili tu. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka na kusimama kwenye karibu na Kigogo kilichopo mbele ya Msikiti na kuuweka mkono wake juu yake huku akiwa anaonekana kama kwamba amekasirika, akauweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto na kuvipitisha vidole vyake vya kulia baina ya vidole vyake vya kulia.

Ambapo Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* hawakuweza kusema chochote kutokana na kumuogopa na kumuheshimu *Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam*. Na wale Masahaba waliokua na Haraka wakaharakisha kutoka Nje, Huku wakiulizana kwa kusema: 'Vipi Leo Sala imefupishwa au?'

Hivyo Kuna Mtu aitwae Dhu Al Yadayn akamsogelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuuliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah Hivi Leo Sala Imefupishwa au umesahau?'

Rasul Allah Sallallahu Alayhi wa Salam **akasema: 'La Haikufupishwa na wala Sikusahau.'**

Dhu Al Yadayn *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama haikufupishwa basi kwa hakika itakua Umesahau.'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akawauliza Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum:*'Hivi Jee Dhu Al Yadayn anasema kweli ama la?'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: 'Naam, anasema Ukweli'
Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasimama. Na kusalisha Rakaa mbili zilizobakia ambazo alizisahau, na kisha akatoa Salam na akasema Allahu Akbar na kusjudu Sijdat ya Sahau ilizochukua mda wa kama Sijda za Kawaida au zaidi kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar na kisha Akasema Allahu Akbar na Kusujud tena Sijda ya pili na kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar.'

Ambapo Imam Muhammad Ibn Sirin alipoulizwa kuhusiana na kua 'Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam kumalizia ama la?'

Basi Imam Muhammad Ibn Sirin akasema kua: 'Mimi nimeambiwa na Imran Ibn Husayn *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoa Salam'*(Bukhari na Muslim)*

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuamrisha kua wale Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walioondoka na kuzikosa Rakaa Mbili zilizofuatia na Sijdat Sahw kua waitwe, waje kusali Rakaa mbili hizo au walete Sijdat Sahw au kusema kua Masahaba hao waambiwe walete Sijda Sahw hio.

Hivyo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua Hua inakubalika kuleta Sijdat Sahw baadaya Kutoa Salam na hua ni Sunnah kufanya hivyo pale itakapokua haukupita mda mrefu kabla Salam hio, wala Mtu husika hajaondoka katika sehemu husika na wala hajazungumza na Mtu yeyote.

Na anasema Imam Abd Rahman Ibn Ahmad Ibn Rajab Al Hanbali katika *Fat-h Al Barr Bi Sahih Bukhari* kua: '**Ama Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Uwajibu wa Sijdat Sahw. Kwani kuna Wanaosema kua ni Wajib ambapo miongoni mwao ni Al Hakam, Ibn Shubramah, Abu Hanifa. Na hii ni kama ilivyonukuliwa na Imam Al Kharki, ambae amenukuliwa na Al Thawri, Ahmad Ibn Hanbal na Is-haq.**

Ambapo hata hivyo Ahmad Ibn Hanbal ameiwajibisha pale tu itakapokua kimetokea kitu ambacho Kitaibatilisha Sala kwa makusudi. Lakini kwa kile ambacho hakitoibatilisha Sala kwa Makusudi basi kama kwa mfano Kuacha Sunnah au kuzidisha Dhikr katika Sehemu sio,isipokua Kutoa Salam katuka sehemu sio, basi Sijdat Sahw hua si Wajibu Kwa maana hio basi kulingana na Mtizamo wa Imam Ahamd Ibn Hanbal basi Sijda Sahw hua si Wajibu, kwa sababu Kusujudu kwa ajili ya Sijda Sahw hua si Wajibu kuifanya wala kuiwacha,ila kuifanya hua ni bora Zaidi.

Kwani imenukuliwa kutoka kwa Imam Malik na Imam Abu Thawr kua; Kama ikiwa ni kutokana na kutotimiza kitu ndani ya Sala basi hua ni Wajib. Na hii ni kwa sababu sehemu yake ya kufanywa hua ni kabla ya Salam.Na hivyo hii huifanya Sijda Sahw kua ni sehemu ya Sala, tofauti na pale inapokua inafanywa baada ya Salam ambapo hua ni baada ya kumalizika Sala.

Ama kwa upande wa Imam Al Shafii basi yeye amesema kua: 'Sijdat As Sahw hua ni Sunnah kwa hali yeyote ile itakavyokua.'

Na kuna Nukuu ambayo imenukuliwa na Imam Ahmad na Wanazuoni wenzake wameitafsiri kumaanisha kuaYeyote anaesema kua Sijdat Sahw kua ni Sunnah, basi humaanisha kua Sala hua haibatiliki kwa kutoitekeleza kwa vyovyote vile itakavyokua. Hivyo huu ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii na pia ndio Mtizamo wa Abd Al Maliki Al Maliki, na ndiohuu pia ndio Mtizamo mwengine wa Imam Abu Hanifa, isipokua kwa upande wake yeye amesema kua:Kama Sijdat Sahw itatekelezwa, basi hua ni yenye kuchukua nafasi ya Wajibu, hata kama ni baada ya Salam.'

Ambapo kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal pia,ana Mitizamo miwili na wa kwanza ni kua Kama Sehemu ya Sijdat Sahw itakua ni kabla ya Salam na kisha ikaachwa kwa Makusudi, basi Sala husika hubatilika.Na kama ikiwa ni baada ya Salam basi kuachwa kwake hakibatilishi Sala, kwa hali yeyote itakavyokua iwe kwa kusahauliwa au kwa makusudi. Na huo pia ndio Mtizamo wa Imam Abu Thawr Al Shafii.*(Fat-h Al Barr Bi Sahih Bukhari)***

Ambapo kwa upande wa Mujtahid Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Yule anaesahau kusjudu kabla ya Kutoa Salam, basi hua ni mwenye kuweza kusjudu baada ya Salam na kisha atasoma Atahiyyat na kisha akatoa Salam tena.'**

Na mbali ya kua kuna uwezekano wa Mtu kua ni mwenye kusahau Sijdat Sahw baada ya kusahau ndani ya Sala, lakini pia kuna hali ya uwezekano wa Kusahau wakati mtu akiwa ndani ya Sijdat Sahw.Hivyo jee Waanzuoni wanasemaje juu yake Jambo hili?

Naam..kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua: '**Anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi Al Shafii kua:Kama ikiwa Mtu atakua ni mwenye Kusahau ndani ya Sijda Sahw na hivyo kua ni mwenye Kusujudu mara Tatu badala ya mara mbili, basi katika hali kama hii hua haihitajiki Kusujudu tena kutokana na kusahau kwake ndani ya Sijda Sahw.'**

'Kwani Al Abadri amenukuu Makubaliano ya Ijmaa ya Wanazuoni yasemayo kua Kama Mtu atasahau ndani ya Sijdat Sahw, basi hatakiwi kusujudu tena kwa kusahau huko. Hivyo kama atakua ni mwenye kua na shaka kama aidha alisujudu mara moja au mara mbili, basi hua anatakiwa aanze kuhesabu kwa idadi ya chini na kisha Asujudu tena,na hivyo itakua wazi kwake kua amesujudu mara mbili, na hana haja ya kuirudia Sijda Sahw.' *(Al Majmuu)*

Na kaa Upande wa Imam Al Muhaqqiin Shaykh Ul Islami Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Kama ikiwa Mtu ataleta Sijda Sahw na kisha akasahau kitu ndani yake labda maneno ya kusema, n.k basi hua hatakiwi kusujudu tena mara ya pili badala yake kwa sababu hua hairuhusiki kufanya kitu hicho hicho kimoja kwa mfuatano wa sambamba.'***(Tuhfah Al Muhtaj)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Al Kasani Al Hanafi kua: **'Kuirudia Sijdat Sahw ndani ya Sala ya Mtu hua hakutuhusiwi, na hii ni kwa sababu kama Mtu amesujudu na kusahau ndani yake, basi kuna uwezekano wa kusahau tena ndani yake na hivyo kupelekea kutokea kaa muendelezo wa Mambo yasiyotakiwa ndani yake'***(Badai Al Sanai)*

Ambapo Mtizamo huo ndio Mtizamo wa Imam Al Sarakhasi Al Hanafi katika Al Mabsut: '**Ama kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi nao wanasema kua, Amesema Imam Malik kua: Mtu yeyote yule atakaekua na shaka ndani ya Sijdat Sahw yake na hivyo kutojua**

kama amesjudu mara moja au mara mbili, basi anatakiwa asujudu mara moja na kisha asome Tahiyyat na atoe Salam, kwanihua hakuna Sijdat Sahw kwa kusahau ndani ya Sijda Sahw.'*(Al Mudawwanah)*

Na kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua: **'Sijdat Sahw kutokana na kusahau ndani ya Sijdat Sahw ni kitu ambacho hakikuamrishwa, kama alivyosema Imam Ahmad, na pia kwa sababu kuna Makubaliano ya Wanazuoni juu ya kutokuwepo kwa Sijdat Sahw kutokana na kusahau ndani ya Sijdat Sahw kama alivyosema Imam Is-haq Ibn Rahawayh,kwani husababisha muendelezo usiokua na mwisho***.'(Sharh Al Kabir)*

Kwa upande mwengine kuna hali nyengine ambayo pia inaweza kutokea ndani ya Sala ya Mtu pale inapokua amekosea zaidi ya Mara Moja, na hivyo ili kulipia Fidya kasoro hizo basi humbidi kuleta Sijdat Sahw.Hivyo jee Hukmu yake huaje?

Naam..imetajwa kwenye *Fiqh Al Manhaj aAla Madhhab Al Imam Al Shafii* kua: '**Sijdat Sahw ni Sunnah ambayo hutekelezwa pale Mtu anapokua ameacha Sunnah Ab'aadh(Sunnah za Wajibu), anapokua na shaka juu ya Idadi ya Rakaa alizosali, inapokua amefanya bila ya kukusudia kitu kisichoruhusiwa ndani ya Sala, na kukosea iwe katika Nguzo za Sala au Sunnah za Wajib au Kitendo cha Hali ya Sala kufanywa katika sehemu ambayo si yake.'***(Fiqh Al Manhaj aAla Madhhab Al Imam Al Shafii)*

Kwa maana hio basi itakapotokea kua Mtu anaesali atafanya Moja kati ya mambo haya yaliyotajwa au zaid ambayo tumesha yazungumzia na kuyafafanua, basi Mtu husika atatakikana kuleta Sijda Sahw.

Ambapo anasema Imam Al Khatib Al Shirbini Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na Sijdat Sahw, hua ni pia kama ikiwa kuna kusahau zaidi mara moja ndani ya Sala.'**

Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliiwekea mipaka Sijdat Sahw kwa Masahaba zake *Radhi Allahu Anhu*m katika Hadith ya Dhu Al Yadayn bila kujali mara ngapi Kasoro imetokeaKwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Alitoa Salam mara mbili, kisha akazungumza na Masahab zake na kisha akatembea.

Hivyo ndani yake kuna vitendo ambavyo alivifanya baada ya kulazimishwa (yaani kujibu aliyoulizwa na Dhu Al Yadayn), na kisha kuna vya kabla yake na baada yake. Hivyo hata kama Mtu atakua ameleta Sijdat Sahw na kisha akakosea kabla ya kutoa Salam, au alisjudu mara tatu,n.k basi hua hatakiwi kusujudu tena kwa sababu akifanya hivyo basi hua si mwenye kua salama kutokana na Uendelevu usiokua na mwisho wa kuleta Sijdat Sahw*(Al Iqna Fi Hal Al Faz Abi Shujaa)***

Kwa maana hio basi Mtu hua anatakiwa alete Sijdat Sahw mara moja tu, hata kama ikiwa alikosea mara tatu ndani ya Sala yake kabla ya kuleta Sijdat Sahw.

Na hata kama ikiwa atakosea ndani ya Sijdat Sahw au atakosema baada ya Kuleta Sijda Sahw na kabla ya Kutoa Salam wakati akiwa ndani ya Sala, basi Sijdat Sahw hio aliyoileta kabla hua ni yenye kumtosheleza kifidia.

Na anasema Imam Sulayman Al Bujaraimi Al Shafii kua: '**Hata kama ikiwa Mtu amezidisha, au amepunguza au amefanya yote na kisha akawa ni mwenye kunuia Kuleta Sijdat Sahw kwa kasoro**

husika basi Sijdat Sahw ya Mtu husika hua ni yenye kufidiya kasoro zote hizo husika, na hivyo hua haina haja ya kuleta Sijdat Sahw kwa Sahw nyengine.' *(Hashiyyah Al Bujaraimi)*

Kwani tumeona kua Sijdat Sahw hua inaletwa pale Mtu anapokua Amepunguza, ameongeza au amekua na shaka na Kitu ndani ya Sala.Ambapo vitu hivyo hua ni vyenye kua ni vya Wajibu kama Nguzo za Sala au Sunnah za Wajib za Sala ambazo tayari tumeshazifafanua.Kwa maana hio Sijdat Sahw hua haikubaliki kuletsa kutokana na sababu ya kua Mtu ameacha Sunna zisizokua za Wajibu ndani ya Sala.

Kwani anasema Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qalyubi Al Masri Al Shafii kua: '**Sijdat Sahw hua haihitajiki kuletwa kutokana na kuachwa kwa Sunna nyenginezo za Sala Hivyo kama Mtu ataleta Sijdat Sahw kwa sababu ya kuacha Sunnah hizo na kwa kukusudia basi Sala ya Mtu huyo hua ni yenye Kubatilika**. **Lakini kama ikiwa ameleta Sijdat Sahw hio bila ya Kujua wala Kukusudia basi Sala yake haibatilik**i.*'(Hashiyyah Al Qalyubi aAla Sharh Ibn Qasim Al Ghazi)*

Na akasema Imam Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Ahmad Al Shafi Al Bajuri kua: '**Kama ikiwa Mtu amefanya Jambo ambalo litampekea kutakiwa kuleta Sijdat Sahw, kwa mfano kutosoma Tahiyyat ya mwanzo na pia jambo ambalo halistahiki kuletewa Sijdat Sahw kwa mfano kutosoma Tasbih na kisha Mtu huyo akaleta Sijdat Sahw kwa ajili ya kuacha mambo yote mawili yanayostahiki kuletewa Sijdat Sahaw na yasiyostahiki**. **Basi Sala yake Mtu huyo itakua ni Batili na hii ni kwa sababu amefanya jambo linalobatilisha Sala ndani yak**e.'*(Hashiyyah Al Bajuri)*

Na anasema Imam Sulayman Ibn Umar Al Jamal Al Shafii katika Hashiyyah Al Jamal aLa Sharh Al Minhaj kua: '**Alivyosema Al Barmawi inamaanisha kua: Inajulikana kua ndani ya Sala kuna Sunnah Ab'adh ambazo hutakiwa kuletewa Sijdat Sahw kama zikiachwa**. **Na kuna Sunnah Haiat Ambazo haitakiwi kuletewa Sijdat Sahw kama zikiachwa, kama vile ambavyo ilivyokua kuhusiana na Adhana na Iqamah ambazo Mtu hua hatakiwi Kuleta Sijdat Sahw kama hakuzisoma pia na hii ni kwa sababu Haikusemwa hivyo.'***(Hashiyyah Al Jamal ala Sharh Minhaj)*

Na Imam Nur Ad Din Ali Shabramilisi Al Shafii anasema pia kua: '**Kwa mfano kama Mtu atakusudia kuleta Sijdat Sahw kwa sababu ya kuisahau Tahiyyat ya kwanza, na pia kwa sababu ya kuacha kusoma Sura baada ya Surat Al Fatiha, na kisha akaleta Sijdat Sahw kwa ajili ya mambo mawili haya Sala yake hua ni Batili.Na hii ni kwa sababu Sijdat Sahw bila ya kua na Sababu hua haikubaliki na imekatazwa. Sasa kutokana na kua Nia ya Mtu husika imechanganya Vitu viwili yaani Wajib na Sunnah, basi kile cha Sunna ndio kinachobatilisha Sala husika.**

Ila kama itakua Alikusudia Kuleta Sijdat Sahw kutokana na kukosea katika moja kati ya mambo mawili haya na hakuweka wazi kua Sijdat Sahw hio ni ya jambo lipi.

Basi hapa inaangaliwa ile hali yenye uzito wa kuhitajika kuletewa Sijdat Sahaw baina ya hali mbili hizi. **Kwa sababu kile kinachohitajika kuletewa Sijdat Sahw hua ni chenye nguvu ya uasili na hivyo kile kisichohitajika kuletewa Sijdat Sahw hua hakihesabiki kwa sababu ya kutokuwepo kwa ubainisho wa wazi baina yao**.'*(Hashiyyah Shabramilisi aAla Nihayat Al Muhtaj)*

Hivyo Hukmu ya Sijdat Sahw hua inazungukia katika Sehemu Kuu Tatu za Sala ambazo ni:

1-Kuacha Kile kilichoamrishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambacho huweza kua ni Nguzo ndani ya Sala husika, hua ni Sunnah Al Ab'aadh au Sunnah Haiat.

Ambapo kuhusiana na Nguzo basi kama ikiachwa kwa Makusudi basi huifanya Sala husika kubatilika. Na kama ikiachwa kwa kusahauliwa, au bila kukusudia basi hubidi kurudiwa na kisha kuleta Sijdat Sahw baada yake, na hii ni kutokana na kua huenda Mtu husika alitekeleza nguzo hio lakini akasahau na hivyo akairudia tena hivyo hua ni Lazima kuleta Sijdat Sahw ili kufidia ziada ya Nguzo husika.

Ama kuhusiana na Sunnah Ab'aadh basi nayo pia hua inahitajia kuletewa Sijdat Sahw pale inapoachwa au kusahauliwa, Iwe kusahauliwa huko ni kwa Hakika au kwa kutokua na hakika kama imesahauliwa ama la.

Ambapo kuhusiana na Sunan Haiat basi hua haihitaji kuletewa Sijdat Sahw, iwe imeachwa kwa Makusudi au kwa kutokusudia. Iwe kuachwa kwake ni kwenye Uhakika kua imeachwa au iwe ni kwenye kua na Shaka kua imeachwa.

Na kwa kua hua haihitaji Sijdat Sahw kutokana na kuachwa kwake basi Mtu akiiletea Sijda Sahw hua ni mwenye kupelekea Kujibatilishia Sala yake.

2-Kufanya Kitendo ambacho kimekatazwa kufanywa ndani ya Ibada ya Sala.

3-Kufanya kitu ndani ya Sala ambacho kitapelekea kuongezea kitu kisichohitajika ndani ya Sala husika, au kusitasita kufanya Jambo husika ndani ya Sala litakalopelekea Sala husika kua na ziada ya kitu husika.

1-Ama tunapoangalia kuhusiana na Kuacha Nguzo ya Sala, basi tunaona kua:

Kama ikiwa Mtu anasali peke yake au Imam anapokumbuka kua amewacha Nguzo yeyote ya Sala isipokua Nia na Takbirat Al Ihram, basi kabla ya kufanya kitu chengine ndani yake hua anatakiwa aitekeleze Nguzo hio hapo hapo, na pia anatakiwa alete Sijdat Sahw mwishoni mwa Sala Kwa sababu ya kuongeza kitu ndani ya Sala kabla ya kutimiza Nguzo husika.

Na hivyo basi kile alichokiongeza baada ya Kuacha Nguzo husika hua hakihesabiki hadi pale atakapotekeleza Nguzo aliyoiruka hapo kabla, kwa sababu miongoni mwa Nguzo za Sala hua pia ni Kufuatisha Utaratibu wake ambao hua hautakiwi kupanguliwa.

Hivyo kama mtu atakua ni mwenye kukumbuka katika Rakaa yake ya mwisho kabla ya kutoa Salam kua aliiruka Sujud katika Rakaa yake hio Basi itambidi Asujudu kisha aanze kusoma Upya Tahiyyat kisha alete Sijdat Sahw na kisha ndio atoe Salam.

Na kama ikiwa amekumbuka katika kisimamo cha Rakaa ya pili kua aliiruka Sujud Moja ya Rakaa ya kwanza na alisimama moja kwa moja basi anatakiwa arudi chini kwenye Kikao, kisha asujudu na pia mwishoni mwa Sala aleta Sijdat Sahw, kwa sababu ya kuzidisha kisimamo ndani ya Sala yake kabla ya Sijda ya pili ya Rakaa husika.

Kama ikiwa Mtu ataruka Nguzo moja au zaidi na kisha akakumbuka katika Rakaa inayofuatia katika kutekeleza Nguzo husika kua kumbe nguzo hizo hakuzitekeleza katika Rakaa iliyotangulia, basi Nguo anazozifanya katika wakati huo itakua ndio Nguzo za Rakaa iliyotangulia. Na hivyo kila kitu kilichotokea baina ya kutotekelezwa kwa nguzo husika ya Rakaa iliyotangulia na Rakaa aliyokuwemo sasa hivi hua hakihesabiki. Na hivyo pia itambidi kuleta Sijdat Sahw Mwishoni mwa Sala yake.

Kama ikiwa Mtu ameruka Sijda Mbili kutoka katika Rakaa ya Mwisho ya Sala yake,basi itambidi Asujudu mara Mbili kisha Asome Tahiyyat na kisha alete Sijdat Sahw.

Kama Mtu akigundua kua ameruka Sijda mbili, kwenye Rakaa aliyokuwepo ndani yake basi atasujudu Sijdat mbili hizo na kisha atakaa Tahiyyat,na kisha ataleta Sijdat Sahw na kutoa Salam. Na kama ikiwa ni za Rakaa iliyotangulia kabla ya Rakaa aliyokuwemo ndani yake basi itambidi airudie Rakaa hio, na kama ikiwa ni kabla ya Rakaa mbili zilizopita na zisizofuatana sambamba kabla yake basi atarudia Rakaa moja tu na kama ni kabla ya Rakaa mbili zilizopita na zinazofuatana sambamba kabla yake, au ana shaka na hana uhakika juu yake basi atarudia Rakaa mbili zote, na kisha ataleta Sijdat Sahw na kutoa Salam.

Kama Mtu akikumbuka kua ameiruka Nguzo ya Sala isiyokua Nia na Takbirat Al Ihram na kisha akakumbuka Mara tu baada ya Kutoa Salam, na kile alichokiruka hakikua cha Rakaa ya mwisho, bali basi itambidi kuirudia Rakaa na kisha kuleta Sijdat Sahw.

Na kama ni Nguzo ya Rakaa ya mwisho basi itambidi arudie nguzo hio kisha amalizie Rakaa hio na mwishoni mwake alete Sijdat Sahw na kisha atoe Salam. **Ambapo Sijdat Sahw hii hua ni kwa ajili ya Usahaulivu ambao umepelekea Kuivunja Nia yake kulikompelekea Kutoa Salam kabla ya kumaliza Sala.**

Na kama ikiwa Mtu ameruka nguzo moja au mbili za Rakaa ya kwanza na ya pili za Sala ya Rakaa Tatu au Nne. Na mara tu baada ya kutoa Salam akakumbuka basi hua anatakiwa hapo hapo, kabla ya kupita mda wowote kunyanyuka na Kuingia kwenye Sala kwa Takbirat Al Ihram bila ya Nia na bila ya Dua ya Ufunguzi wa Sala. Kisha baada ya Takbirat Al Ihram, atasoma Surat Al Fatiha na kisha atarudia Rakaa kulingana na alichokifuta na kisha atakaa katika Tahiyyat ya mwisho ataleta Sijdat Sahw na kisha atatoa Salam.

Kwani amesema Muhammad Idris Al Shafii kua: **'Yeyote yule atakaetoa Salam, au akazungumza bila ya kukusudia, au akasahau kitu chochote kile muhimu ndaniya Sala yake, basi anatakiwa aendelee na Sala, pale inapokua Mtengano bado haujawa mkubwa'***(Al Bayyan)*

Ambapo kuhusiana na urefu wa Mtengano wa Muda wa Tukio basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wametofuatiana ambapo kuna wanaosema kua Urefu na Ufupi wa kupita hua unategemeana na Dasturi na utamaduni wa Jamii ya watu husika kwa namna wanavyochukulia urefu na ufupi wa wakati wa kitu na hivi ndivyo ilivyopelezewa na Imam Al Shafii katika Kitab Al Umm ambao ndio pia mtizamo wa Imam Ali bin Ahmad al-Bandaniji Al Shafii.

Na Mtizamo wa pili ni usemao kua mda husika uwe si wenye kuzidi Zaidi ya mtu kua ni mwenye kusali Rakaa moja ambayo ni ya kusoma Surat Al Fatiha tu ndani yake ambao huu ni mtizamo wa Imam Al Buwayti, Imam Abu Is-haq Al Marwazi.

Na mtizamo wa Tatu ni wa Imam Al Mutawali na Imam Al Qaffal Al Shashi usemao kua Kiasi cha Mtengano wa Mda ni kama ilivyopokewa katika Hadith Dhu Al Yadayn *Radhi Allah Anhu* usiwe mdogo wala usiwe mkubwa zaidi yake.*(Al Bayyan)*

Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Hali hii ya Kukumbuka baada ya Salam, basi kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii hua inaruhusika kuingia kwenye Sala na kumalizia lakini pale inapokua katika kukumbuka huko hayajayokea mambo matatu yafuatayo:

1-Iwe haujapita Mda mrefu baada ya Salam.

2-Iwe Mtu hajazungumza na Mtu hajazungumza na Mtu yeyote.

3-Iwe Mtu hajageukia upande mwengine usiokua ni wa Kibla.

Ambapo hii hua ni kulingana na kama ilivyofafanuliwa na Hadith ya Dhu Al Yadaynisemayo:

عن أبي هُرَيرَة رَضِيَ اللهُ عَنْه، قال صلَّى بنا رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم إحْدَى صلاتَيِ العشيِّ – سمَّاها أبو هريرة، ولكن نسيتُ أنا– قال: فصلَّى بنا ركعتينِ، ثم سلَّمَ، فقام إلى :قال ابن سِيرين خشبةٍ معروضةٍ في المسجِدِ، فاتَّكأَ عليها كأنَّه غَضبانُ، ووضَعَ يَدَه اليُمنى على اليُسرى، وشبَّكَ بين أصابعِه، ووَضَع خَدَّه الأيمنَ على ظَهرِ كفِّه اليُسرى، وخرَجتِ السَّرَعانُ من أبوابِ المسجدِ، فقالوا: وعُمرُ، فهابَا أن يُكلِّماه، وفي القومِ رجلٌ في يديه طولٌ، يُقال قَصُرتِ الصَّلاةُ؟ وفي القومِ أبو بكرٍ له: ذو اليَدينِ، قال: يا رسولَ الله، أَنسيتَ أمْ قَصُرَتِ الصَّلاةُ؟ قال: لم أَنسَ ولم تَقصُر! فقال: أكَمَا يقولُ ذو اليدين؟ فقالوا: نعَمْ، فتقدَّم فصلَّى ما تَرَك، ثم سَلَّم، ثم كَبَّر وسجَدَ مِثلَ سُجودِه أو أطولَ، ثم رفَعَ رأسَه وكبَّر، ثم كبَّر وسَجَد مِثلَ سجودِه أو أطولَ، ثم رفَع رأسَه وكبَّر. فربَّما سألوه (أي: سألوا ابنَ سيرينثم سلَّم؟ فيقول: نُبِّئتُ أنَّ عِمران بن حُصَينٍ، قال: ثم سَلَّمَ

Amesema Muhammad Ibn Sirin kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitusalisha moja kati ya Sala za Jioni (Ambapo Imam Ibn Sirin anasema kua Abu Hurayrah Aliitaja Sala hio ila mimi nimeisahau) na akaihitimisha Sala hio baada ya Kuisalisha kwa Rakaa mbili tu. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka na kusimama kwenye karibu na Kigogo kilichopo mbele ya Msikiti na kuuweka mkono wake juu yake huku akiwa anaonekana kama kwamba amekasirika, akauweka mkono wake wa kulia juu ya mkono wa kushoto na kuvipitisha vidole vyake vya kulia baina ya vidole vyake vya kulia.

Ambapo Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* hawakuweza kusema chochote kutokana na kumuogopa na kumuheshimu *Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam*. Na wale Masahaba waliokua na Haraka wakaharakisha kutoka Nje, Huku wakiulizana kwa kusema: 'Vipi Leo Sala imefupishwa au?'

Hivyo Kuna Mtu aitwae Dhu Al Yadayn akamsogelea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumuuliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah Hivi Leo Sala Imefupishwa au umesahau?'

***Rasul Allah Sallallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La Haikufupishwa na wala Sikusahau.'**

Dhu Al Yadayn *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama haikufupishwa basi kwa hakika itakua Umesahau.'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akawauliza Masahaba zake** ***Radhi Allahu Anhum:*****'Hivi Jee Dhu Al Yadayn anasema kweli ama la?'**

Masahaba ***Radhi Allahu Anhum*** **wakasema: 'Naam, anasema Ukweli'**

Hivyo ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akasimama. Na kusalisha Rakaa mbili zilizobakia ambazo alizisahau, na kisha akatoa Salam na akasema Allahu Akbar na kusjudu Sijdat ya Sahau ilizochukua mda wa kama Sijda za Kawaida au zaidi kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akbar na kisha Akasema Allahu Akbar na Kusujud tena Sijda ya pili na kisha akanyanyua kichwa na kusema Allahu Akba**r.'

Ambapo Imam Muhammad Ibn Sirin alipoulizwa kuhusiana na kua 'Jee ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alitoa Salam kumalizia ama la?'**

Basi Imam Muhammad Ibn Sirin akasema kua: 'Mimi nimeambiwa na Imran Ibn Husayn ***Radhi Allahu Anhu*** **kua** ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alitoa Salam'***(Bukhari na Muslim)*

Ama kuhusiana na Nia na Takbirat Al Ihram basi ikiwa Mtu amesahau zote au Amesahau Nia au Takbirat Al Ihram basi hua ni Lazima airudie Sala yote nzima iwe kukumbuka kwake ilikua ndani ya Sala au baada ya Sala, iwe umeshapita mda mrefu ama la.

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Tumesema hapo kabla kua Sala hua haikamiliki bila ya Takbirat Al Ihram, hivyo kama Mtu akisali bila ya Nia au au bila ya Takbirat Al Ihram basi Sala yake hua Batili.Hivyo kama Imam au Maamuma ameiwacha kwa makusudi au kwa kusahau basi Sala yake hua ni Batilina hakuna kitakachomsaidia kuifanya Sala yake hio kua isibatilike'**

'Huu ndio Mtizamo wetu, mtizamo wa Abu Hanifa, Malik Ahmad, Abh Daud na wengi miongoni mwa Wanazuoni Kwani amesema Al Shafii kua Mtu akiwasalisha watu bila ya Takbirat Al Ihram basi Sala yao hua Batili'*(Sharh Al Muhadhdhab)*

Na amesema Imam Malik kua: '**Kama Mtu atawasalisha Watu bila Takbirat Al Ihram kutokana na kusahau hadi mwisho wa Sala, basi hua hakuna Sala kwa Imam wala kwa Maamuma'***(Al Mudawwana)*

Na akasema Imam Ibn Qudamah kua: '**Takbirat Al Ihram ni moja kati ya Nguzo za Sala Hivyo yeyote yule atakaesali bila ya Takbirat Al Ihram iwe kwa kukusudia au bila ya kukusudia basi Sala yake hua ni Batili na huu ndio pia Mtizamo wa Rabiah, Malik, Ath Thawry,Al Shafii, Is-haq, Abh Thawr na Ibn Al Mundhir**i'*(Al Mughni)*

Kwa maana hio basi unaweza kuleta Sijdat Sahw kuacha Nguzo nyenginezo za Sala na kuzirudia, lakini kamwe huwezi kuleta Sijda Sahw kwa sababu ya kuacha Nia au Takbirat Al Ihram. Kwa sababu yote uliyoyafanya ulikua umeyafanya kabla ya kuingia ndani ya Sala.

Na kama tulivyosema kua Malengo ya Sijdat Sahw hua ni kulipa Fidiya ya Kasoro zilizotokea ndani ya Sala.Hivyo kwanza unatakiwa uingie ndani ya Sala kwa Nia na Takbirat Al Ihram na kisha kama utasahau baada ya hayo basi ndio utaleta Sijdat Sahw.

Na kama tulivyosema kua Malengo ya Sijdat Sahw hua ni kulipa Fidiya ya Kasoro zilizotokea ndani ya Sala, Kwani hio ni kuhusiana na Nia ya Takbirat Al Ihram, kwani kuna hadith isemayo:

حَدَّثَنَا سُوَيْدُ بْنُ سَعِيدٍ، حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ مُسْهِرٍ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ، طَرِيفٍ السَّعْدِيِّ ح وَحَدَّثَنَا أَبُو كُرَيْبٍ، مُحَمَّدُ بْنُ الْعَلاَءِ حَدَّثَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ السَّعْدِيِّ، عَنْ أَبِي نَضْرَةَ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ، عَنِ النَّبِيِّ ـ صلى الله عليه وسلم ـ قَالَ " مِفْتَاحُ الصَّلاَةِ الطُّهُورُ وَتَحْرِيمُهَا التَّكْبِيرُ وَتَحْلِيلُهَا التَّسْلِيمُ

Amesema Suwaidu Ibn Said kua amesema Aliyyu Ibn Mus-hir kua amesema Abi Sufyan kua amesema Taririf Ibn Saidi kua amesema Abi Nadhrat kua amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Ufunguo wa Sala ni Udhu, Kuingia ndani yake ni kwa Allahu Akbar na kuifunga kwake ni kwa Salam*(*Sunnan At Tirmidhii, Sunnan Abu Daud,Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo asema Imam Al Muhaqiqin Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii. '**Kwa maana hio basi Kama Mtu atasahau Kutoa Salam, lakini akakumbuka kabla haujapita Mda basi mtu huyo atatoa Salam na haitokua na haja kwake kuleta Sijdat Sahw, kwa sababu sehemu ya Sijdat Sahw hua imeondoka baada ya kutolewa Salam.Lakini kama mda utakua umeshapita basi itambidi kuirudia upya Sala yake hio.'***(Tuhfah Al Muhtaj Fii Sharh Al Minhaj)*

Na hivyo hivyo pia alivyosema Mujaddid Ad Din Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii katika kuifafanua hadithya Dhu Al Yadayn *Radhi Allahu Anhu* pale aliposema kua: '**Hadith inatuonesha kukubalika kuendelezwa kwa Sala kwa yule Mtu ambae ametoka nje ya Sala bila ya kukusudia**. **Ambapo ndani yake inajumuisha hukmu ya kua Mtu anaetoka nje ya Sala bila ya kukusudia hua si mwenye kukatisha Sala yake***(Fath Al Barr)*

Lakini kama Mtengano wa tukio utakua mrefu kiwakati, labda tuseme Mtu ameshaondoka katika sehemu aliyosalia. **Hadith inatuonesha kukubalika kuendelezwa kwa Sala kwa yule Mtu ambae ametoka nje ya Sala bila ya kukusudiaAmbapo ndani yake inajumuisha hukmu ya kua Mtu anaetoka nje ya Sala bila ya kukusudia hua si mwenye kuhitajia Takbirat Ihram kurudi ndani yake, na kua Nia na Salam ya kutokea Nje ya Sala (kwa kusahau) hua si yenye kumkatishia Sala yake**

Hivyo kama Mtengano wa tukio utakua mrefu kiwakati, labda tuseme Mtu ameshaondoka katika sehemu aliyosalia, au ameshatokwa na udhu basi katika hali kama hii Sala yake hua imebatilika kwa sababu ya kukosekana Salam ya kutokea ndani ya Sala, na hivyo mtu husika itambidi kuirudia upya Sala hio.

Na amesema Imam Ibn Juzzay pia kua: '**Kama Mtu atasahau kutoa Salam na mda ukawa umeshapita au Udhu umeshamtoka basi sala yake mtu huyo hua ni Batili.'**

Ambapo hapa nataka tufahamiane kua Hali Tunayoizungumzia hapa ni hali ya kua Mtu hakutoa Salam kabisa. Na hatuzungumzii kuhusiana na Mtu ambae ametoa Salam Moja tu, Kwa sababu kama tulivyosema hapo kabla kua: '**Kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni basi ni kua Taslim ya kwanza ha ni Wajib Lakini Taslim ya Pili hua ni Sunnah.'***(Imam An Nawawi katika Al Majmuu)*

Ambapo Mujtahid Imam Al Muhammad Idris Shafii amesema kua: '**Aina Fupi kabisa ya Taslim hua ni ASalaam Alaykum, hivyo mtu akikosema herufi basi anarudia tena kutoa Salam, na kama**

hakufanya hivyo wakati yupo mwisho wa Sala basi anasujudu Sijdat Sahw na kisha aseme ASalaam Alaykum.'*(Al Umm)*

Na amesema Mujtahid Imam Abu Bakr Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua: '**Kutoka kwa Wanazuoni wote niliosoma kutoka kwao basi ni wenye kusema kua Sala ya Mtu mwenyeKutoa Salam moja hua ni Sahih.'**

HUKMU YA KUA NA SHAKA NDANI YA SALA

❖❖❖

Naam, miongoni mwa Hadith zenye kuelezea kuhusiana na Hukmu ya kua na shaka ndani ya Ibada ya Sala na nini cha kufanya ikitokea hivyo ni kama hadith zifuatazo:

حَدَّثَنَا أَبُو يُوسُفَ الرَّقِّيُّ، مُحَمَّدُ بْنُ أَحْمَدَ الصَّيْدَلاَنِيُّ حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ سَلَمَةَ، عَنْ مُحَمَّدِ بْنِ إِسْحَاقَ، عَنْ مَكْحُولٍ، عَنْ كُرَيْبٍ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ عَوْفٍ، قَالَ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ يَقُولُ " إِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ فِي الثِّنْتَيْنِ وَالْوَاحِدَةِ فَلْيَجْعَلْهَا وَاحِدَةً وَإِذَا شَكَّ فِي الثِّنْتَيْنِ وَالثَّلاَثِ فَلْيَجْعَلْهَا ثِنْتَيْنِ وَإِذَا شَكَّ فِي الثَّلاَثِ وَالأَرْبَعِ فَلْيَجْعَلْهَا ثَلاَثًا ثُمَّ لْيُتِمَّ مَا بَقِيَ مِنْ صَلاَتِهِ حَتَّى يَكُونَ الْوَهْمُ فِي الزِّيَادَةِ ثُمَّ يَسْجُدْ سَجْدَتَيْنِ وَهُوَ جَالِسٌ قَبْلَ أَنْ يُسَلِّمَ

Amesema Abu Yusuf Al-Raqqi kua, Muhammad bin Ahmad Al-Saydlani amesema kua, Muhammad Ibn Salamah amesema kua, kutoka kwa Muhammad Ibn Ishaq, kutoka kwa Makhoul, kutoka kwa Kurayb. Kutoka kwa Ibn Abbas kua amesema Abd Rahman Ibn Awf *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Nimemsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema kua: Kama ikitokea miongoni mwenu kua Mtu amesahau ndani ya Sala yake na hajui kama amesali Rakaa Moja au Mbili, basi wacha ahesabie kwenye Rakaa moja, na kama hajui kama ni Rakaa Tatu au Nne basi na ahesabie kua ni Rakaa tatuNa kisha asujudu Mara Mbili kabla ya Kutoa Salam.' *(Imam At Tirmidhii,Sunan Ibn Majah)*

Na amesema Imam Abu Daud kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ الْعَلَاءِ ، حَدَّثَنَا أَبُو خَالِدٍ ، عَنِ ابْنِ عَجْلَانَ ، عَنْ زَيْدِ بْنِ أَسْلَمَ ، عَنْ عَطَاءِ بْنِ يَسَارٍ ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ ، قَالَ : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : إِذَا شَكَّ أَحَدُكُمْ فِي صَلَاتِهِ فَلْيُلْقِ الشَّكَّ ، وَلْيَبْنِ عَلَى الْيَقِينِ ، فَإِذَا اسْتَيْقَنَ التَّمَامَ سَجَدَ سَجْدَتَيْنِ ، فَإِنْ كَانَتْ صَلَاتُهُ تَامَّةً كَانَتِ الرَّكْعَةُ نَافِلَةً وَالسَّجْدَتَانِ ، وَإِنْ كَانَتْ نَاقِصَةً كَانَتِ الرَّكْعَةُ تَمَامًا لِصَلَاتِهِ ، وَكَانَتِ السَّجْدَتَانِ مُرْغِمَتَيِ الشَّيْطَانِ ، قَالَ أَبُو دَاوُدَ : رَوَاهُ هِشَامُ بْنُ سَعْدٍ ، وَمُحَمَّدُ بْنُ مُطَرِّفٍ ، عَنْ زَيْدٍ ، عَنْ عَطَاءِ بْنِ يَسَارٍ ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَحَدِيثُ أَبِي خَالِدٍ أَشْبَعُ

Amesema Muhammad Ibn Aalai kua aamsema Abu Khalid kua amesema Aajlan kua amesema Zayd Ibn Aslam kua amesema Ataa Ibn Yasir kua amesema Abu Said Al Khudhry *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

'Kama mmoja wenu atakua na Shaka ndani ya Sala yake,basi na aikanushe Shaka hio na kisha Asimamie juu ya Yaqini. Na kisha anapokua na Yaqini katika Kumaliza Sala yake basi na Asujudu Mara mbili. Hivyo kama ikiwa Sala imekamilika, basi Rakaa iliyongezeka hua ni Sunnah na Sijda mbili hua ni Sunna. Na ikiwa Sala haikukamilika basi Rakaa aliyoiongeza hua ni yenye kukamilishia Sala yake na Sijda mbili hua ni kwa ajili ya Kumuadhirisha Shaytan.'*(Sunan Abu Daud)***

Na pia amesema Ibrahim kua

عن عبد الله بن مسعود رضي الله عنه قال: صلى النبي صلى الله عليه وسلم –قال إبراهيم: لا أدري زاد أو نقص– فلما سلم قيل له: يا رسول الله، أَحَدَثَ في الصلاة شيء؟ قال: «وما ذاك»، قالوا: صليتَ كذا وكذا، فَثَنَّى رِجليْهِ، واستقبل القبلة، وسَجَدَ سجدتين، ثم سلم، فلما أقبل علينا بوجهه، قال: «إنه لو حَدَثَ في الصلاة شيءٌ لَنَبَّأْتُكُم به، ولكن إنما أنا بَشَرٌ مثلكم، أنسى كما تَنْسَوْن، فإذا نسَيتُ فذَكِّرُوني، وإذا شَكَّ أحدكم في صلاته، فَلْيَتَحَرَّ الصَّوَابَ فليُتِمَّ عليه، ثم ليسلم، ثم يسجد سجدتين

Amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisalisha.

Kisha Ibrahim anaendelea kusema kua: 'Sijui kama alizidisha au alipunguza Rakaa za Sala. Ila Abd Allah Ibn Masud alisema kua : Baada ya kutoa Salam ya kumalizika Sala basi *Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam* aliulizwa: 'Jee kuna kitu kipya kimeongezeka Ndani ya Sala Ya *Rasul Allah?'*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza: 'Kwanini Mnauliza hivyo?'**

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: Kwa Sababu Umesalisja Rakaa Kadhaa w Kadhaa

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakalia Miguu yake na kuelekea Kibla na Kisha akaleta Sijda Mbili na kisha akatoa Salam. Na kisha baada yake akageuka na kutuelekea sisi Masahabazake na akasema:

'Kama ingekua Kuna kitu kimeongezwa ndani ya Sala basi bila ya shaka ningelikuambieni. Ila mimi ni (Bashara) Mtu kama Nyinyi na hua nnasahau kama mnavyosahau, Hivyo nitakaposahau basi nikumbusheni.

Na Yeyote yule Miongoni mwenu atakapokua na Shaka juu ya Sala yake, basi na asimamie kile kilicho sahih kwake na kisha amalizie Sala yake ipasavyo, na kisha atoe Salam kisha Asujudu mara mbili'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Naam tumeangalia Hadith tatu zenye kuzungumzia kuhusiana na Hukmu ya kua na Shaka ndani ya Ibada ya Sala ambazo ni Hadith ya Abd Rahman Ibn Awf *Radhi Allahu Anhu* iliyomo kwenye Sunnan Ibn Majah na Imam At Tirmidhii.Hadith ya Abu Said Al Khudry *Radhi Allahi Anhu* katika Sunan Abu Daud.Na Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* katika Bukhari na Muslim.

Na kama zilivyosema kua kama Mtu atakua na shaka basi anatakiwa asimamie katika kile alichokua na Yakini nacho katika Sala yake, na kisha alete Sijdat Sahaw.Kwa sababu kuongeza hua ni bora kuliko kupunguza.

Ambapo amesema Imam Ibn Ahu Bakr Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua: **'Hadith ya Abu Said Al Khudhr ndio Hadith Sahih zaidKuhusiana na Suali hili.'**

Ambapo kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi basi anasema kua: '**Imam Al Shafii na Wanazuoni wengineo Waliowengi ni wenye kusimamia katika Mtizamo wa kwamba, ikiwa Mtu ana shaka kwa mfano juu ya Rakaa alizosali ni Tatu au Nne basi kwanza mtu husika anatakiwa Ajenge Yakini ambayo itakua ni yenye kusimamia mtizamo wenye Idadi ndogo kabisa,hivyo akamilishe Sala yake kisha alete Sijdat Sahw.'***(Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo kwa upande wa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi tunaona kua wao wanasema kua: '**Mtu atakaekua ni mwenye kusali na kisha kua na shaka juu ya Idadi ya Rakaa alizosali, basi hua ni bora kuanza mwanzo. Na kama itakua ni vigumu basi na akisie, kulingana na itakayokua ni Idadi ya chini kabisa.'**

Na hii ni kwa sababu Wanazuoni wametofautiana katika kuzifahamu na kuzifafanua Hadith tatu hizi, ambapo kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wametafsiri kua kwa Mtu atakea kua na shaka kwa mara ya kwanza ndani ya Sala yake basi itambidi ajaribu kurekebisha kwa kufanya lililosahih lakini pale masuali yanayoleta Shaka kua mengi zaidi ndani ya Sala.Na hivyo basi hua inaruhusika kuanza mwanzo upya Sala husika kutokana na Shaka.

Mbali ya kua Kulingana na Mtizamo wa Imam Al Shafii na Wanazuoni wengineo kua inatakiwa kwanza kua na Yakini juu ya Rakaa husika.

Ambapo maana ya ya neno **Shaka hua ni kua na Hisia za Kutokua na uhakika na hivyo mtu kua ni (Huwa Turadid Bayna Imrayni) mwenye kusitasita baina ya mambo mawili ambapo miongoni mwao mambo hayo basi hakuna lenye Faida zaidi juu ya jengine.**

Hivyo kwa upande wa Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Malik Ibn Anas, Imam Muhammad Idris Al Shafii basi wanasema kua: '**Mtu anapokua na Shaka Ndani ya Sala basi na asimamie katike lile alilokua na hakika nalo.'** Na hii ni kulingana na Hadith ya Ataa Ibn Yasir kupitia kwa Abu Said Al Khudhry *Radhi Allahu Anhu.*

Na kwa upande wa Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Abu Hanifa na Imam Al Awzai basi wao wanasema kua: '**Mtu anapokua na Shaka ndani ya Sala yake basi na achunguze na kisha asimamie juu ya kile anachokiona kua kunakaribiana na Usahih.'**Na hii ni kulingana na Uthibitisho wa Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu.*

Ama kwa upande wa Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Malik na Imam Al Shafii basi wao wakasema kuhusiana na Uthibitisho wa upande wa Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Abu Hanifa na Imam Al Awzai kua: '**Maana ya maneno yasemayo basi Mtu na achunguze hua yanamaanisha kua ni yenye**

kumtaka mtu husika kua na Nia juu ya kilichokua Sahih na hivyo kuupata Uyakini juu ya kitu husika. Kama vile alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Asisali mmoja wenu katika Wakati linapochomoza Jua au Linapozama Jua.'*(Imam An Nasai)*

Kwa maana hio basi Hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* hua ni kama Ufafanuzi wa Hadhith ya Abd Rahman Ibn Awf *Radhi Allahu Anhu.*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Shawkani basi yeye amesema kua: '**Kwangu mimi badi naona kua hakuna kutofautiana baina ya Hadith zenye kusemakua Mtu na Asimamie katika Hali ya Yaqini na zisemazo kua Mtu asimamie katika Idadi ya chini kabisa kwani zote hizi zinamtaka Mtu husika kuchunguza ili apate kile kinachokaribiana na usahih.**

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha kusimamia kwenyw Idadi ndogo ya kitu na kua na Yakini juu ya kitu pale mtu anapokua na Shaka juu ya kitu husika. Hivyo kama itawezekana kuachana na Shaka kwa kuchunguza, na hivyo Mtu akaweza kujua Amesali Rakaa ngapi kutokana na kua ni mwenye Yakini, basi bila ya Shaka kuhakikisha kwa Yakini hua kwenye kupewa kipaumbele zaidi kuliko kusimamia Udogo wa Kiidadi.

***Kwa Sababu Allah Subhanah wa Ta'ala* ametoa chaguo la kuhesabu kwa Idadi ndogo kwa ajili ya wale wasioweza kujua kama ilivyosemwa kwenye Hadith ya Abd Rahman Ibn Awf *Radhi Allahu Anhu.*Kwani kwa yule mwenye kujua na kufanya Uchunguzi huweza kua na Hakika kutokana na Yakini kama ilivyosema Hadith ya Abu Said Al Khudhry.**

Hivyo yule mwenye kuhitimisha kwa Yakini huhitimisha kwa Alichokua na Uhakika nacho, na hivyo hii ni yenye kuonesha kua Hadith hizi hazipingani.'*(Nail Al Awtar)*

Ama Tunapozungumzia kuhusiana na Shaka ndani ya Sala basi hua kuna hali zifuatazo ambazo zikitokea hua zinatakiwa zisitiliwe maanani:

1-Kama ikiwa ni hali ya Shaka ya Kuzuka tu isiyokua na msingi wowote.

2-Kama ikiwa ni hali ya Shaka yenye kujirudia rudia kwa Mtu ambae kila akifanya Ibada basi lazima awe na shaka ndani yake.

3-Kama ikiwa ni hali ya Shaka ambayo mtu imemjia baada ya kumaliza kusali, ambapo hapa atatakiwa asimamie katika kile alichokifanya na kua na uhakika nacho.

Kwani Kulingana na Sharia za Kiislam basi Inapokua kuna Shaka juu ya Kitu basi Athari yake hua haifanyi kazi pale inapokua Kuna Uhakika wa Yakini juu ya Kitu husika.Kwani Kile chenye Uhakika hua hakibatiliki isipokua kwa kuwepo Uhakika mwengine utakaothibitisha vyenginevyo.

Na Wanazuoni katika Kufafanua kwao kuhusiana na Shaka Ndani ya Sala basi wamefafanua pia kwa njia ya Kumithilisha kuhusiana na Kua na Shaka katika Talaka.

Ambapo Kisharia kuhusiana na Talaka basi Kama Mwanamme ana shaka kuhusiana na kua alitamka Talaka Ama la, basi Hukmu yake hua ni kua kama anavyosema ImamAbu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Bahadir Al Zarkashi Al Shafii kua: '**Kama Mume atakua na shaka kuhusiana na kua alitamka au hakutamka maneno ya Talaka, basi Sharia hua haisimamii Athari ya Shaka na hivyo hua haiuondoi Uyakini**. **Na kutokana na kua Maisha ya Ndoa baina ya Mume**

na Mke hua ni yenye kusimamia Msingi wa Yakini, na kila chenye Yakini hua hakibatilishwi na chengine chochote isipokua Yakini nyengineo.'*(Al Manthur fi Qawaid Fiqhiyyah)*

Na akasema Imam Muhammad Alau Ad Din Al Haskafi Al Hanafi kua: '**Kama Mume aliapa lakini hajui kama alichoapia ilikua ni Talaka ama ni kitu chengine basi Talaka hio hua ni Batili.'***(Darr Al Mukhtar)*

Na akasema Imam Ibn Qudamah Al Hanbali kua: '**Kama Mume atakua hajui kama kaumuacha Mkewe ama la, basi hali ya Shaka hii ua Talaka hua haiuondoi Uhakika wa kuwepo kwa ndoa.'***(Al Mughni)*

Na akasema Imam Al Khatib Al Shirbini kua: '**Kama ikiwa Mume atakua na shaka kama alitamka Talaka ama la, basj kwa upande wetu sisi Mashafi hatuhesabu kua Talaka imetolewa, Na Al Muhammad amesema kua: Kuna Makubaliano ya Ijmaa juu ya hilo kwa sababu Kanuni ya Fiqh inasema kua Talaka haikutoka na Ndoa haijabatilika.'** *(Al Mughni Al Muhtaj)*

Na akasema Imam Al Kharashi Al Maliki kua: '**Kuna Tofauti baina ya Shaka juu ya Najis na Juu ya Talaka**. **Kwani Shaka katika Talaka hua inabatilika lakini hua haibatiliki katika Udhu.**

Na hii ni kwa sababu Shaka juu ya Najisi inahusiana na Kusimamia Hukmu ya Asili ya Ibada ya Sala. **Hivyo Mtu hawezi kuingia ndani ya Sala isipokua pale asipokua na Shaka juu ya Tohara yake yaani atakapokua na uhakika wa Udhu wake**. **Lakini tunapozungumzia kuhusiana na Talaka basi hua inahusiana na Kuvunja Hukmu ya Asili.**

Kwani Uasili wa Hukmu Ndoa ni kua na Mke na Kuruhusika Kuingiliana nae Kimwili, ambako hua hakubatilishwi na kua na Shaka.*(Sharh Al Mukhtasar Al Khalil)*

Hivyo kwa maana hio basi Kama Mtu alisali hadi akamaliza na kutoa Salam, na kisha ndio akajiuliza kwa kua na Shaka ya kua Sijui alisali sawasawa au alipunguza au alizidisha Rakaa ndani ya Sala yake hio, basi anatakiwa aachane na Shaka hio na wala asiitilie Maanani kwa sababu Ibada yake husika imeshamalizika,na hivyo Uhakika wa Ibada yake hua hauwezi kubatilika kutokana na Athari ya Shaka hio.

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu kua:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَلَا تُبۡطِلُوٓاْ أَعۡمَٰلَكُمۡ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo ateeAAoo Allaha waateeAAoo alrrasoola wala tubtiloo aAAmalakum *(Surat Muhammad 47:33)*

Tafsir: ***Enyi Wale ambao Mlioamini Mtiini Allah na Mtiini MtumeNa Wala Msizibatilishe Amali zenu.***

Hivyo kwa kua Mtu husika Tayari ameshamaliza kuifanya Ibada ya Sala husika basi hua haina haja kwake kuibatilisha kutokana na kua na shaka baada yake.Ambapo shaka tunazozungumzia hapa hua ni kuhusiana na Kua na shaka kuhusiana na yaliyotokea ndani ya Sala kama kayatekeleza ama la baada ya kumaliza Sala.

Ila Tunapozungumzia kuhusiana na kua na Shaka juu ya Nia ya Sala au Takbirat Al Ihram, basi katika hali kama hii Sala husika hua ni Batili na ni kwa sababu Mtu husika Hakuingia kwenye Sala hapo kabla, kwani Nia na Takbirat Al Ihram ndio Ufunguo wa Sala. Na kama huna uhakika kama ulifungua Mlango wa sehemu na kisha ukaingia ndani yake basi utapojikuta Uko nje yake hua inamaanisha kua hukuingia ndani yake.

Na Amesema Imam Muhammad Idris Al Shafi kua: 'Kama ikiwa Mtu amekua na shaka kuhusiana na kama ametia nia katika Sala yake ya fardhi ama la, na kisha baada ya hapo akakumbuka kua naam ametia nia, basi kama shaka hii ilimjia kabla yakufanya cchochote ndani ya Sala yake, basi anaweza akaendelea kusali na Sala ikawa Sahih, lakini kama ikiwa amekumbuka baada ya kua tayari ni mwenye kufanya vitendo vya Sala, basi Sala yake hio hua ni Batili' *(Al Bayyan Fii Madhhab Shafii)*

Kwa maana hio basi Mtu akiwa na Shaka juu ya Nia ya Sala na Takbirat Al Ihram kama alizitekeleza ama la Basi Mtu huyo humbidi kuanza upya Ibada ya Sala yake hio. Na Itambidi kuirudia Sala, bila kujalisha kama Shaka yake hio ilimjia katika wakati akiwa ndani ya Sala au baada ya kutoka ndani ya Sala.

Na kama inatokea kwa Mtu kua ni mwenye Tatizo la kua na shaka mara kwa mara ndani ya Sala yake, basi mtu husika anatakiwa kua ni mwenye kujitahid kumuomba *Allah Subhanah wa Ta'ala* ammpe ulinzi dhidi ya Shaytani.

Kwa sababu mara nyingi sana Shaka hua inasababishwa na Shaytani kumtia wasiwasi Mtu afanyae Ibada.

Na kama Shaka Ikiwa imekujia baada ya Sala, basi itakubidi kudharau shaka hio.

Na usiruhusu kujitia shaka na Kubatilisha Sala yako kutokana na hisia za kua umekosea na hivyo kutaka kurudia rudia Ibada yako, kwani kutoa Fursa hio kutampelekea Shaytani kukuchezea zaidi kiufahamu kwa kukutia wasiwasi zaidi na hivyo kukuharibia maisha yako.Kwani katika Ibada hua inahitajika kua na Msimamo wenye Uiamara na Uhakika wa Yakini.

عن أبي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قال : قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : يَأْتِي الشَّيْطَانُ أَحَدَكُمْ فَيَقُولُ : مَنْ خَلَقَ كَذَا ؟ مَنْ خَلَقَ كَذَا ؟ حَتَّى يَقُولَ: مَنْ خَلَقَ رَبَّكَ ؟ فَإِذَا بَلَغَهُ فَلْيَسْتَعِذْ بِاللَّهِ وَلْيَنْتَهِ.

Kwani amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salllahu Alayhi wa Salam* kua: '**Shaytani hua ni Mwenye Kumjia mmoja miongoni mwenu na na kumwambia, Jee ni Nani alieumba kitu kadhaa na kadhaa? Nani alieumba kadhaa na kadhaa? Huendelea hadi kufikia kuuliza kua Ni Nani aliemuumba Mola wako?. Hivyo akifikia hali hio basi Wacha Mtu huyo aombe hifadhi kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha asite wasiwasi.'** *(Bukhari na Muslim)*

Ambapo kutokana na hadith hii basi Wanazuoni wametoa Hukmu isemayo kua: '**Mtu yeyote mwenye Wasiwasi Mkubwa au shaka ya mara kwa Mara katika Ibada basi na azidharau Shaka hizo'**

Kama alivyosema Mujaddid Ad Din Al Hafidh Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Maana ya maneno ya hadith hii yasemayo kua "Wacha Mtu huyo aombe Hifadhi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha asitishe Shaka hio, yanaamanisha kua:Mtu huyo anatakiwa arudi kwa Allah**

Subhanah wa Ta'ala kumuomba Amkinge na Wasiwasi na Shaka hizo kwani zinataka kumuangamizia Majukumu yake Kiibada na na Kiufaham kutokana na Minong'onezo hio ya Shaytan Hivyo Mtu husika anatakiwa kwa uwezo wake wote kuyasukuma na kutoa Shaka hizo kwa kufanya Jambo jengine badala yake.'*(Fat-h Al Bar)*

Ambapo kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anasema kua: '**Maana ya maneno hayo ni kua Mtu husika anatakiwa kuachana na Mawazo hayo yaliyokua sio na kisha arudi kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kumuomba amuondolee shaka hio**.'*(Sharh Sahih Muslim)*

Kwani Shaka au Wasi Wasi hua ni wa hali za aina tatu:

1-Kua na Shaka juu ya Kitu bila kujua kua hisia hio ni shaka au Wasiwasi.

2-Kua na Shaka ya kukisia kutokea kwa kitu ambacho hakikutokea na hivyo kuhukumu kua kimetokea.

3-Kua na Shaka au Wasi wasi mara kwa mara kama kwamba ni Kawaida au ni Tabia yake Mtu, ambayo haya hua ni Maradhi.

Ambapo anasema Imam Al Muhaqqiqin, Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: '**Tofauti baina ya Wasiwasi na Shaka hua ni kwamba Shaka hutokana na Dalili.**

Kwa mfano Mtu kuachana na nguo za Mtu ambae ni mwenye kawaida ya kugusa Najis, na kuachana na kusali nyuma ya Mtu ambae ni mwenye kawaida ya kutojali Tohara ya Nguo zake. Na kwa kua hali ya Asili ya kitu kumaumbile hua ni Tohara. Ambayo hata hivyo katika hali kama hii hua ni yenye kupingika kutokana na kutawaliwa na Najis ya mara kwa mara kikawaida na hivyo hua kunatakikana Tahadhari.

Hivyo hali hii hua ni tofauti na Wasiwasi kwani Wasiwasi hua ni Kutoa Hukumu ya kitu kua na Najisi bila ya kua na Dalili.

Jambo ambalo hua si lenye kupingana na hali ya Asili ya Kitu, yaani hua ni sawa na Mtu kununua Nguo mpya na kisha Kutaka kuifua kabla ya kuivaa kama tahadhari. Na hivyo hii hua ni Bidaa kama alivyosema An Nawawi katika Sharh Al Muhadhdhab. Hivyo katika hali kama hii hua inatakikana kuachana na Tahadhari. Kwa sababu Mtu mwenye Wasi wasi hua ni mwenye kukisia kitu ambacho hakijatokea lakini yeye akahukumu kua kimetokea, kwa mfano kufikiria kua Najisi imeangukia kwenye nguo yake, na kisha kuhukumu kua nguo imenajisika bila ya yeye kua na Ushahidi wa kuwepo kwa Najisi hio*(Fatawa Al Fiqhiyyah Al Kubra)***

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekataza kufuata yale yenye shaka pale aliposema katika Qur'an kua:

﴿وَمَا لَهُم بِهِۦ مِنۡ عِلۡمٍۚ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا ٱلظَّنَّۖ وَإِنَّ ٱلظَّنَّ لَا يُغۡنِي مِنَ ٱلۡحَقِّ شَيۡـٔٗا﴾

Wamā lahum bihi min ʿil'min in yattabiʿūna illā l-ẓana wa-inna l-ẓana lā yugh'nī mina l-ḥaqi shay-an*(Surat AnNajm 53:28)*

Tafsir: **Wakati wakiwa hawana Ilm kutokana naloNa Hivyo ni wenye Kufuata DhanaNa Kwa Hakika ya DhanaHaiwezi kabisa Kuchukua Nafasi ya Hakika hata Kidogo**.

Hivyo basi Shaka hua haihesabiki pale inapotokea baada ya Mtu kufanya Ibada Husika, yaani kama Sala kwani Shaka hua Kamwe haiwezi kuchukua Nafasi ya Hakika au Yakini. Na Shaka hio hua ni ya bure kwa sababu hua ni yenye kuhesabiwa kua ni yenye kutokana na Mnong'ono wa Shaytani.

Ila kama shaka itatokea ndani ya Ibada ya Sala husika basi hua inabidi kufanyiwa kazi kabla ya kumalizika Ibada ya Sala husika.

Ambapo amesema Al Muhaqqiq Ibn Aabidin Ash Shami Al Hanafi kua: '**Mtu mwenye Shaka sana hua anatakiwa akikate chanzo cha Wasiwasi huo na wala asitilie maanani shaka na wasiwasi huo kwa sababu hua ni kutokana na Shaytani na sisi Tumeamrishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kupingana nae tena na tena.'**

Na akasema Imam Al Mardawi kua: '**Kwa mtu mwenye kua na Shaka na Wasiwasi katika wakati wa Ibada ya Sala yake kiasi ya kufikia kua ana wasiwasi sana, basi anatakiwa aachane na Shaka hizo kwa sababu hua ni usumbufu kwake kua anaona amesali Rakaa nyingi zaidi mbali ya kua ni mwenye hakika kua amesali sawasawa n.k.**

Basi kwa mtu kama huyu hua anatakiwa asitilie maanani Shaka hizo iwe katika Sala, katika Udhu, katika Kukoga Kogo kubwa au kujitoharisha,n.k.'*(Al Insaaf)*

Ambapo kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Al Muhaqqiqin Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii basi yeye anasema baada ya kuulizwa kuhusiana na Tiba ya Shaka na Wasi wasi kua: '**Naam..Ipo tiba yake ambayo ni Mujarrab sana na hii hua ni kuyadharau tu Mawazo hayo yanayokusababishia Shaka na Wasiwasi, hata kama itakua kuna uzito juu yake ndani ya Nafsi yako.**

Na hii ni kwa sababu kama Mtu akiwa hakuyatilia Maanani mawazo ya Shaka na Wasiwasi huo Basi hayatokua na Msingi wa kubakia nae, bali yataondoka baada ya mda mfupi tu, kama vile walivyofanikiwa juu yake wale waliofuzu.

Ama kwa wale aatakaokaa na kuyasikiliza na kuyaendekeza basi Shaka na Wasi wasi hua utaongezeka ndani ya Ufahamu wake hadi kufikia kumtia Wazimu. **Na hua ni zaidi ya Wazimu kama vile tulivyoona kwa wale wenye kuyasikukiza na kuyaendekeza na kudhuriwa nayo na kudhuriwa na Shaytani wake pia Na katika Sahihatayn kua kile kinachounga mkono hiki nikichokitaja pale ziliposema Hadith kua:**

Yeyote atakaekua na Shaka na Wasiwasi basi na aamini kua ni upotovu na hivyo aombe hifadhi dhidi yake kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha asitishe Wasiwasi huo.

Hivyo Tafakkar manufaa ya Dawa hii iliyofundishwa na yule ambae asiesema kwa matamanio yake. **Kwa ajili ya Ummah wake na kisha fahamu kua alienyimwa kitu kutoka kwake Basi amenyimwa Mema wote.**

Kwani Wasiwasi na Shaka hua ni kutoka kwa Shaytan kama tunavyokubaliana. **Na hakuna malengo yeyote ya Shaytan isipokua kumfanya Muumini aangukie kwenye shimo la Upotovu, Maangamizo, mchanganyo wa akili na kiza cha Roho yake hadi atakapofanikiwa kumtoa kwenye Imani ya Dini ya Kiislam.**

Na Mtu husika Hua hahisi kua Shaytani ni Adui yake, Hivyo Mfanyeni Shaytan kua ni Adui yenu Na imetajwa kwenye Hadith kua: Yeyote yule atakaehisi kua amekumbwa na maradhi ya Wasiwasi basi na aseme *Ana Amana Bi Allahi Wa Rasulihi* - Mimi namuamini Allah na Mitume wake.

Kwani hakuna shaka ya kua yeyote yule mwenye kukumbuka Njia za Mitume wa A*llah Subhanah wa Ta'ala* hususan Mtume wetu *Salallahu Alayhi wa Salam,*basi ataona kua njia zake na sharia zake ni nyepesi sana, zilizokua wazi na safi na zenye vithibitisho vya wazi bila ya ugumu wowote ndani yake.

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuweka uzito kwenye Dini, na yeyote atakaetafakari haya na kuyaamini kwa Imani ya kweli basi Maradhi ya Wasiwasi, shaka na minong'ono ya Ibilisi itatoweka kutoka kwake.

Na amesema An Nawawi baada ya kunukuu kutoka kwa baadhi ya Wanazuoni kua: '*Inapendekezwa kwa mtu mwenye Maradhi ya Wasiwasi na Shaka katika wakati sa Kutia Udhu na katika Kusali kwake, basi na aseme*La Ilaha Illah Allah* Kwa sababu Shaytan anaposikia Dhikr hii hua ni mwenye kujitenga na kukimbia.Kwani *La Ilaha Illa Allah* ndio mwanzo wa Dhikr, na Imesemaa kua Dawa Mujarrab ya kutibu Wasiwasi na Shaka hua ni Kuingia kwa umakini kwenye Dhikr Allah na kuirudia mara kwa mara.'*(*Fatawwah Fiqhiyyah Al Kubra)*

Kwani Imai ya Dini ya Kiislam ni nyepesi Sana kiasi ya kua hakuna mtu anaetakiwa kuhisi kua anafanyiwa uzito ndani ya Dini yake au kua na shaka ndani yake, kama ilivyoema hadithi ifuatayo:

روى البخاري في صحيحه عن أبي هريرة، عن النبي صلى الله عليه وآله وسلم قال: «إِنَّ الدِّينَ يُسْرٌ، وَلَنْ يُشَادَّ الدِّينَ أَحَدٌ إِلَّا غَلَبَهُ، فَسَدِّدُوا وَقَارِبُوا، وَأَبْشِرُوا، وَاسْتَعِينُوا بِالْغَدْوَةِ وَالرَّوْحَةِ وَشَيْءٍ مِنَ الدُّلْجَةِ.

Imepokewa na Imam Al Bukharikatika Sahih yake kuaamesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*kua: **'Kwa hakika Dini ni Nyepesi, na hakuna mtu yeyote anaeifanya Dini kua ngumu isipokua Itamuangamiza yeye mwenyewe, hivyo kuweni wenye msimamo wa Kati na kati, jitahidi kwa kadri mtakavyoweza na furahieni!(Ibada zenu) Na ombeni msaada(Kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala*) Asubuhi, na mchana na baadhi ya wakati wa Usiku.**'

Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Shaka zinazohusiana na Ibada ya Sala basi kama tulivyoona kua kama Shaka itatokea baada ya Kumalizika kwa Ibada ya Sala basi Shaka hio hua haina athari yeyote kwa Sala husika.

Lakini tunapozungumzia kuhusiana na Shaka ambazo zitatokea ndani ya Sala basi tunaona kua zimegawika katika sehemu ambazo baadhi hua zina Athari na hivyo kuibatilisha Sala na baadhi hua hazina Athari yeyote juu ya Sala husika na haziibatilishi Sala lakini hua inatakiwa zisimamiwe kulingana na zisemavyo Hukmu za Sharia. Na pia kuna zisizokua na athari na hivyo haziibatilishi Sala na hua haina haja kusimamiwa na Hukmu za Sharia juu yake.Na ifuatayo ni baadhi ya mifano ya athari hizo na utatuzi wake:

Shaka Ambayo Haina Athari yeyote - Hii hua ni Shaka ambayo haiibatilishi Sala na wala haihitaji kupitishiwa Hukmu yeyote juu yake. **Na Aina hii ya Shaka hua ni pale inapotokea hali zifuatazo:**

Kwanza Pale inapokua Mtu anasali na kisha akajikuta anasoma *Tahiyyat* ya Mwisho, au tayari ameshamaliza *Tahiyyat* ya mwisho, huku akiwa na shaka kuhusiana na Rakaa hio aliyojikuta ndani yake.Na hivyo hajui kama hio ni *Tahiyyat* ya Rakaa ya pili ama la na jee Tahiyyat hio inastahiki kuwepo ndani yake ama la?Au amemaliza Rakaa ya kwanza na hivyo kaingia kwenye *Tahiyyat* hio kimakosa ama la?.

Hivyo katika hali kama hii basi Mtu husika atatakiwa kujihesabia kua ameshasali Rakaa mbili, na hivyo *Tahiyyat* hio ni yenye kustahiki kwenye sehemu yake aliyokuwepo.Na hivyo atakapomaliza *Tahiyyat* hio basi atasimama na kumalizia Rakaa ya Tatu kama ni Sala ya Rakaa tatu, au atamalizia Rakaa ya Tatu na nne Kama hio ni Sala ya Rakaa nne.

Ama kama ikiwa Sala hio ni Sala ya Rakaa mbili basi Ataimalizia *Tahiyyat* hio kama *Tahiyyat* ya mwisho na kisha atatoa Salam na Sala yake itakua Sahih, na haina haja ya Sijdat Sahw.

Au Pale mtu anaesali Sala ya Rakaa Nne na kisha akajikuta kua anasoma *Tahiyyat* au ameshamaliza kusoma *Tahiyyat*. Huku akiwa na uhakika kua ameshaipita Rakaa ya pili lakini hana uhakika kuhusiana na Rakaa aliyokuwepo.Yaani kama ndio ameshamaliza Rakaa ya Nne, na Hivyo *Tahiyyat* hio ni Stahiki alipoisoma ama la, au yuko kwenye Rakaa ya Tatu na hivyo *Tahiyyat* hio haistahiki kusomwa alipoisoma?

Hivyo Mtu anapojikuta katika hali kama hii basi hua anatakiwa kuihesabu Rakaa aliyojikuta ndani yake kua ni Rakaa ya Nne, na hivyo atamalizia *Tahiyyat* yake na kutoa Salam na Sala yake itakua Sahih na hatotakiwa kuleta Sijdat Sahaw.

Na pia Pale Mtu anaesali Sala ya Rakaa tatu, na akajikuta anasoma *Tahiyyat* ya Mwisho au ameshamaliza kuisoma na anatoa Salam.Lakini akajikuta ana shaka ya kuhusiana na Rakaa hio kama ni ya Tatu ama la, na Jee Tahiyyat inastahiki hapo alipojikuta ndani yake ama la?

Basi katika hali kama hii Mtu husika anatakiwa ajihesabu kua ameshasali Rakaa tatu na hivyo atatakiwa kutoa Salam na Sala yake itakua Sahih na Hatohitajika kuleta Sijdat Sahw.

Hivyo kuna Shaka ambazo zina Athari na hivyo kuibatilisha Sala na baadhi hua hazina Athari yeyote juu ya Sala husika na haziibatilishi Sala lakini hua inatakiwa zisimamiwe kulingana na zisemavyo Hukmu za Sharia. Na pia kuna zisizokua na athari na hivyo haziibatilishi Sala na hua haina haja kusimamiwa na Hukmu za Sharia juu yake.

Ambapo miongoni mwa shaka ambazo zinabatisha Sala ni kama tulivyosema kua kwa Mtu aliesahau Nia na Takbirat Al Ihram, na mambo mengineyo ambayo tutayazungumzia kwenye sehemu ya mambo yanayobatilisha Sala.

Ama kuhusiana na Shaka zenye Athari lakini hazibatilishi Sala basi kama zisimamiwa kisharia hua ni kua na Shaka juu ya utekelezwaji wa Mambo ya Wajib ambaho yanatakiwa kuletewa Sijdat Sahw kama tulivyoona hapo kabla.

Na kuhusiana na shaka zisizokua na Athari na hazibatilishi Sala basi hua ni kuhusiana ya yale yaliyokua ni Sunnah, kama vile kua na uhakika wa kuacha Tasbih katika wakati wa kurukuu na kusujudu. Kua na shaka juu ya kuacha kitendo ambacho hakiko wazi, kua ni Sunnah au Wajib, kua na shaka ya kucha kitu kinachopenekezwa,n.k ambapo kutoleta Sijdat Sahw kutokana na kua na shaka ya kuyasahau haya hua ni bora kuliko kuleta Sijdat ya Sahw kutokana na kua na uhakika kua umeyawacha.

Na aimetajwa katika Fat-h Al Aziz kua: **‘Kama ikiwa mtu atakua na shaka yakua amepangua mpangilio ama la basi hua haina haja ya kuleta Sijdat Sahw kama vile ambavyo mtu anavyokua ana shaka ya kua amesahau ama la, na ama ikiwa mtu anashaka ya kua ame amefanya jambo lisilotakikana ndani ya Sala yake, kwa mfano kua anashak aya kua amezungumza ndan yake ama la au aametoaSalam akwa kusahau ama la basi kikanunihapa hua inahesabia kua hakufany akitu hicho.’***(Fat-h Al Aziz)*

Ama kwa upandewa kuhusiana na ulazima na kutokua na ulazima wa Sijdat Sahw kwa Maamuma anapokua Nyuma ya Imam hua nipale inapokua katika hali zifuatazo:

Kwanza ingawa Sijdat Sahw ni Sunnah kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii lakini kwa upande mwengine basi tunaona kua Sijdat Sahw hua pia ni Fardhi lakini ni katika Hali moja Tu.Ambayo ni pale Mtu anapokua Maamuma na kisha Imam akaleta Sijdat Sahw, basi katika Hali hii Sijdat Sahw hua ni Fardhi kwa Maamuma husika kuitekeleza na hivyo Itambidi amfuate Imam wake, kwani kama hakumfuata basi Sala yake Maamuma itakua ni Batili.

Ila Hukumu hii hua haifanyi kazi pale itakapokua Maamuma anajua Kosa la Imam wake katika kusahau kwake ndio kulikompelekea kuleta Sijdat Sahw, Lakini Maamuma akawa na uhakika kua Imam huyo hakusahau kitu.

Hivyo Imam akaleta Sijdat Sahw lakini Maamuma akawa hakumfuata basi hua hakuna tatizo, ambapo hii ni katika hali hii tu.

Kwani Kama Ikiwa Imam atakosea au atasahau na kisha kwa makusudi au kwa kukosea au kwa kusahau akawa hakuleta Sijdat Sahw au aliamua kuileta baada ya Salam, basi kwa upande Maamuma atatakiwa kuleta Sijdat Sahw baada ya Salam ya Imam na kabla ya Salam yake yeye. Maamuma hua hatakiwi kuleta Sijdat Sahw kama itakua yeye ndie aliesahau ndani ya Sala yake, wakati akiwa nyuma ya Imam, kwa sababu Imam ndie anaebeba usahaulivu wa Maamuma kutokana na kua yeye ndie anaeongoza Sala.

Ambapo Hukmu hii inatokana na Mfano wa Tukio la Muawwiyah Ibn Al Hakam *Radhi Allahu Anhu* alipomtakia Rehma za *AllahSubhanah wa Ta’ala*Mtu alieenda chafya wakati wakiwa Wanasali Nyuma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m, na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema Baada ya Sala kua: Sala hua haitakiwi kua na Maneno ya Mazungumzo ya Watu ndani yake.

Kama ilivyoelezewa kwenye hadith ifuatayo:

حَدَّثَنَا أَبُو جَعْفَرٍ، مُحَمَّدُ بْنُ الصَّبَّاحِ وَأَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ – وَتَقَارَبَا فِي لَفْظِ الْحَدِيثِ – قَالاَ حَدَّثَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، عَنْ حَجَّاجٍ الصَّوَّافِ، عَنْ يَحْيَى بْنِ أَبِي كَثِيرٍ، عَنْ هِلاَلِ بْنِ أَبِي مَيْمُونَةَ، عَنْ عَطَاءِ بْنِ يَسَارٍ، عَنْ مُعَاوِيَةَ بْنِ الْحَكَمِ السُّلَمِيِّ، قَالَ بَيْنَا أَنَا أُصَلِّي، مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم إِذْ عَطَسَ رَجُلٌ مِنَ الْقَوْمِ فَقُلْتُ يَرْحَمُكَ اللَّهُ . فَرَمَانِي الْقَوْمُ بِأَبْصَارِهِمْ فَقُلْتُ وَاثُكْلَ أُمِّيَاهْ مَا شَأْنُكُمْ تَنْظُرُونَ إِلَىَّ . فَجَعَلُوا يَضْرِبُونَ بِأَيْدِيهِمْ عَلَى أَفْخَاذِهِمْ فَلَمَّا رَأَيْتُهُمْ يُصَمِّتُونَنِي لَكِنِّي سَكَتُّ فَلَمَّا صَلَّى

رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَبِأَبِي هُوَ وَأُمِّي مَا رَأَيْتُ مُعَلِّمًا قَبْلَهُ وَلاَ بَعْدَهُ أَحْسَنَ تَعْلِيمًا مِنْهُ فَوَاللَّهِ مَا كَهَرَنِي وَلاَ ضَرَبَنِي وَلاَ شَتَمَنِي قَالَ " إِنَّ هَذِهِ الصَّلاَةَ لاَ يَصْلُحُ فِيهَا شَىْءٌ مِنْ كَلاَمِ النَّاسِ إِنَّمَا هُوَ التَّسْبِيحُ وَالتَّكْبِيرُ وَقِرَاءَةُ الْقُرْآنِ

Wamehadithia Abu Ja'far, Muhammad Ibn al-Sabbah, na Abu Bakr Ibn Abi Shaybah ambao walikuwa sawa katika maneno ya Hadith - walisema, Ismail Ibn Ibrahim, kwa mamlaka ya Hajjaj al-Sawwaf, kutoka kwa Yahya Ibn Abi Kathir, kutoka kwa Hilal bin Abi Maimunah, kutoka kwa Ata Ibn Yassar, kutoka kwa Muawiyah Ibn Al-Hakam Al-Sulamiy *Radhi Allahu Anhu*amesema: Nilipokuwa nikisali pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Kuna Mtu mmoja miongoni mwa watu alipiga chafya, nami nikasema:*Yarhamuka Allah!*

Hivyo watu wakanitazama kwa mtizamo wa kutopendeza, nami nikasema: 'Naapa kwa Masikini Mama yangu, Nimefanya nini mbona mnanitizama hivyo?'. Watu hao wakaanza kupigapiga mapaja yao, na nilipoona kua wananiashiria kukaa kimya basi nikaingiwa na hasira lakini nikakaa kimya.

Na baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumaliza kusali basi mimi sikuwahi kuona kiongozi bora katika kutoa maelekezo zaidi yake kabla yake ambae nnaweza kumtlea muhanga Mama yagu na Baba yangu kwa ajili yake, kwani Wallahi hakunidhihaki, wala hakunipiga na wala hakunitukana bali alisema: 'Na kwa hakik katika Sala hii hakuna kitu chochote kinachohusiana na Mazungumzo ya kawaida ya watu, bali ndani yake mnajumuishwa kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Kumsifu*Allah Subhanah wa Ta'ala,*kusoma Qur'an na mambo kama hayo.'

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumwambia Muawwiyah Ibn Al Hakam kua airudie Sala yake, wala kua aleta Sijdat Sahw.

Ambapo mfano mwengine ni kua tusema Maamuma wakati anasalishwa katika Tahiyyat ya mwisho basi akadhania kua amemsikia Imam ametoa Salam na hivyo nae akatoa Salam, lakini kumbe Imam hakutoa Salam.

Basi katika Hali kama hii Basi Maamuma hua anatakiwa kubakia ndani ya Sala yake hadi pale Imam atakapotoa Salam na kisha nae atoe Salam.Na Maamuma huyu hatostahiki kuleta Sijdat Sahw kwa sababu alifanya kitendo kutokana na kusahau wakati akiwa anaongozwa na Imamu wake ndani ya Sala.

Au pale itakapokua Maamuma ambae amechelewa na Kuwakuta Watu washamtangulia kwa Rakaa moja au kadhaa.Na hivyo akaunganisha Jamaa na katika kusali kwake katika Tahiyyat ya mwisho ya Jamaa basi yeye Akasikia kua Imam katoa Salam, na hivyo yeye akanyanyuka kumalizia Rakaa zilizobakia, Lakini kumbe Imam hakutoa Salam.

Na tuseme Labda Maamuma huyo akawahi kumalizia Rakaa yake na akagundua kua kumbe Imam hakutoa Salam. Hivyo katika Hali kama hii basi Maamuma atarudi chini na kuendelea kusubiri hadi Imam atoe Salam kisha atamalizia Rakaa yake bila kuleta Sijdat Sahw.

Na kama aliwahi kumalizia hio Rakaa kabla ya Salam ya Imam, basi Rakaa hio kwake itakua haihesabiki kwa sababu alikua bado yupo chini ya Uongozi wa Imam wake, na hivyo atarudia Rakaa hio tena baada ya Salam ya Imam na pia haitomhitajia kuleta Sijdat Sahw.

Lakini kama itakua Imam huyo atawahi kutoa Salam kabla ya Maamuma huyo hajarudi chini, basi hapa Itambidi Maamuma Arudi chini, kisha amalizie Rakaa yake na kisha alete Sijdat Sahw kwa sababu ya kosa la Kuongeza kitendo ndani ya Sala baada ya Imam kutoa Salam.

Na kama ikiwa Maamuma amesahau baada ya Imam kutoa Salam kwa Maamuma aliechelewa, basi hapa Imam hua habebi kasoro ya usahaulivu wa Maamuma kwa sababu Uimamu wake mbele ya Maamuma wake umeshakatishwa.*(Fiqh Ibadat fi Madhhab Shafii)*

Kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An-Nawawi Al Shafii kua: **'Kama Imam ataleta Sijdat moja tu kwa ajili ya Sijdat Sahw, basi kwa yule atakaekua anasali nyuma yake itambidi alete na Sijda Sahw ya pili yake, huku akiwa ni mwenye kua na mtizamo kua Imam amekosea. Hivyo kama Imam hakusjudu Sijdat Sahw kwa makusudi au amesahau basi Maauma wake anatakiwa aelete Sijdat Sahw. Na huu ndio mtizamounaokubalika zaidi miongoni mwa Wanazuoni kwa sababu kukosea kwa Imam hua kunazifanya kua na kasoro Sala za wanaomfuata Nyuma yake kutokana na usahaulivu wake. Hivyo Kama Imam hakuletaSijdat Sahw kulipia fidia kasoro yake basi yule anaemfuata hua ni wajibu wake kuleta Sijdat Sahw kwa ajili ya kujilipia fidia Sala yake.'**

'Hivyo kama Imam akiwa amefanya makosa katika Sala yake na kisha ikawa hakuleta Sijdat Sahw basi msimamo sahih kulinganana Madhhab yetu ni kua yule anaesali Nyuma yake Imam anatakiwa kuleta Sijdat Sahw hio na huu ndio pia mtizamo wa Ahmad, Ibn Al Mundhir ambae amenukuu kutoka kwa Ibn Sirin, Al Hakam na Qatadah. 'Ata, Al Hasan, an-Nakha'i, Al Qasim, Hammad Ibn Abi Sulayman, Ath-Thawri, Abu Hanifah, Al Muzani, na Ahmad ambae pia ana mtizamo mwengine ambao ni kua Maamma hua hatakiwi kuleta Sijdat Sahw katika hali kama hii.'*(Al Majmuu)*

YALIYORUHUSIKA NDANI YA SALA - JUU AU NDANI YA KIPANDO

❖❖❖

Ama kuhusiana na yale yasiyobatilisha Sala kama kugeuka mara moja, kuchukua hatua moja au mbili za Miguu, kuangalia kitu kitakachomtolea Mtu Umakini wa Sala, Kukumbuka Kitu chengine ndani ya Sala kama ilivyoonesha Hadith tuliyoanza nayo ya Uqbah Ibn Harith *Radhi Allahu Anhu* basi hua hakumpelekei Mtu kutakiwa kuleta Sijdat Sahw ambayo inasema kua:

حَدَّثَنَا إِسْحَاقُ بْنُ مَنْصُورٍ، حَدَّثَنَا رَوْحٌ، حَدَّثَنَا عُمَرُ ـ هُوَ ابْنُ سَعِيدٍ ـ قَالَ أَخْبَرَنِي ابْنُ أَبِي مُلَيْكَةَ، عَنْ عُقْبَةَ بْنِ الْحَارِثِ ـ رضى الله عنه ـ قَالَ صَلَّيْتُ مَعَ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم الْعَصْرَ، فَلَمَّا سَلَّمَ قَامَ سَرِيعًا دَخَلَ عَلَى بَعْضِ نِسَائِهِ، ثُمَّ خَرَجَ وَرَأَى مَا فِي وُجُوهِ الْقَوْمِ مِنْ تَعَجُّبِهِمْ لِسُرْعَتِهِ فَقَالَذَكَرْتُ وَأَنَا فِي الصَّلاَةِ تِبْرًا عِنْدَنَا، فَكَرِهْتُ أَنْ يُمْسِيَ أَوْ يَبِيتَ عِنْدَنَا فَأَمَرْتُ بِقِسْمَتِهِ

Amesema Is-haqa Ibn Mansuri kua amesema Rawhu kua amesema Umar Ibn Said kua amesema Ibn Abi Mulaikat kua amesema Uqbah Ibn Al Harith *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Nilisali Sala ya Al Asr pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na hivyo mara tu baada ya Kutoa Salam basi alinyanyuka haraka sana na akaelekea katika moja kati ya Makazi ya Wake zake na kisha akatoka.

Na alipotoka *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi akagundua hali ya mshangao kwenye Nyuso za Watu kutokana na Kasi ya mwendo wake Hivyo akasema: Nilikumbuka wakati nikiwa katika Sala Yangu kuhusiana na Kipande cha Dhahabu bacho kilikuwepo Nyumbani kwangu. Nami nikawa sikupenda kua Kipande hicho kibakie na sisi Ndani ya Usiku wa leo, hivyo nimeamrisha kua kigaiwe Sadaka.'*(Sahih Bukhari)***

Ambapo Mfano mwengine wa Hadith zinazoainisha matukio yasiyohitajia kuletewa Sijdat Sahw juu yake ni kama ilivyosema Hadith ya U*mmu Ul Muuminina* Aisha *Radhi Allahu Anha*aliposema kua:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، حَدَّثَنَا سُفْيَانُ بْنُ عُيَيْنَةَ، عَنِ الزُّهْرِيِّ، عَنْ عُرْوَةَ، عَنْ عَائِشَةَ، قَالَتْ صَلَّى رَسُولُ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ فِي خَمِيصَةٍ لَهَا أَعْلاَمٌ فَقَالَ " شَغَلَنِي أَعْلاَمُ هَذِهِ اذْهَبُوا بِهَا إِلَى أَبِي جَهْمٍ وَائْتُونِي بِأَنْبِجَانِيَّتِهِ.

Amesema Abu Bakr Ibn Abi Shaybah kua amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Al Zuhri kua amesema Urwat kua Aisha *Radhi Allahu Anha* amesema: '*Rasul Allaaah Salallahu Alayhi wa Salam* alisali kwenye *Khamisaa* (Msala uliotengenezwa kwa Manyoya ya Ngozi ya Mbuzi au Sufi wenye michoro michoro) na hivyo katika Sala yake hio akawa ni mwenye kuangalia Michoro yake hio. Na baada ya Sala akasema: 'Iondoe Khamisa hii mpelekee Abu Jahm na kisha niletee *Inbijaniyah* (Msala wa Sufi usiokua na michoro) kwani *Khamisaa* hii imeniondolea Khushuu yangu ndani ya Sala.''*(Imam Al Bukhari)***

Ambapo mfano mwengine ni Hadith ya Abu Qatadah *Radhi Allahu Anhu* ambayo inasema kua:

حَدَّثَنَا أَبُو الْوَلِيدِ، حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، حَدَّثَنَا سَعِيدٌ الْمَقْبُرِيُّ، حَدَّثَنَا عَمْرُو بْنُ سُلَيْمٍ، حَدَّثَنَا أَبُو قَتَادَةَ، قَالَ خَرَجَ عَلَيْنَا النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم وَأُمَامَةُ بِنْتُ أَبِي الْعَاصِ عَلَى عَاتِقِهِ، فَصَلَّى فَإِذَا رَكَعَ وَضَعَهَا، وَإِذَا رَفَعَ رَفَعَهَا

Amesema Abu Al Walidi kua amesema Al Layth kua amesema Said Al Maqburiyyu kua amesema Amr Ibn Sulami kua amesema Abu Qatadah*Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikuja Upande wetu (Msikitini) huku akiwa amembeba Umamah ambae ni Mtoto wa Abi Al As Juu ya Mabega yake, na kisha Akasali na alipokua anataka Kurukuu akamuweka chini Mtoto huyo na alipokua akinyanyuka akamnyanyua Mtoto huyo.' *(Sahih Muslim)*
Ambapo tunapoziangalia Hadith tatu hizo zote basi tunaona kua hakuna hata moja iliyosema kua kisha baada yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaleta Sijdat Sahw.

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kuhusiana na Hadith hii ya Abu Qatadah*Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutokana**

na Rehma na Huruma zake kwa Watoto alimbeba Umamah na kumuweka Mabehani na kusali nae na aliporukuu alimuweka Chini ili asije Akaanguka katika Kurukuu na Kusujudu kwake, na kutokana na kutotaka kukosa amani na utulivu juu ya Mtoto huyo baada ya Kusujudu basi aliamua kumbeba tena. **Na Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akifanya yote hayo kwa ajili ya kufundisha kua inaruhusika kufanya hivyo kwenye Sala.'***(Fat-h Al Barr)*

Hivyo kwa wale wenye Watoto wadogo ambao hawawezi kuwaacha peke yao na hakuna mtu wa kuwaachia na mda wa Sala umewadia basi hua inaruhusika kufanya kama alivyofanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwani hakukubatilishii Sala yako na wala huyotakiwa kuleta Sijdat Sahw na wala hutokua na Wasi wasi kuhusiana na Usalama wa Mtoto pale inapokua hakuna wa Kumuachia.

Ama kuhusiana na kukumbushana pale Mtu anapokosea ndani ya Sala yake basi hua inaruhusika kwani anasema Imam Abu Abd Allah Muhamad Ibn Saad Ibn Mani Al Zuhri Al Basri kua: '**Amesema Imam Muhammad Ibn Sirin kua: Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alifikia wakati ikawa anasahu ndani ya Sala yake**. **Hivyo ili kutatua tatizo hilo la Usahaulivu ndani ya Sala.Basi Umar Ibn Al Khattab Radhi Allahu Anhu akaamua kumteua Mtu maalum kwa ajili ya kua ni mwenye Kusimama Nyuma yake na kumfuatilia katika kusali kwake ili kama akisahau ndani yake basi awe ni mwenye Kumkumbusha***(Kitab Tabaqat Al Kabir)*

Ambapo Kisa hiki pia kimetajwa na Imam Ahmad Ibn Yahya Ibn Jabir Al Baladhuri Katika Kitabu chake cha Al Ansab Al Ashraf.

Na hii ni kwa Sababu hata *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Aliamrisha kufanya hivyo kama ilivyoelezewa katika Imam Ibn Khuzaymah katika Sahih yake ambae anasema kua:

مُحَمَّدُ بْنُ يَحْيَى، ثنا الْحُمَيْدِيُّ، ح وَثنا مُحَمَّدُ بْنُ عَمْرِو بْنِ تَمَّامٍ الْمِصْرِيُّ، نا يُوسُفُ بْنُ عَدِيٍّ قَالَا: ثنا مَرْوَانُ بْنُ مُعَاوِيَةَ، عَنْ يَحْيَى بْنِ كَثِيرٍ الْكَاهِلِيِّ، عَنْ مِسْوَرِ بْنِ يَزِيدَ الْأُسَيْدِيِّ، وَقَالَ مُحَمَّدُ بْنُ يَحْيَى الْأَسَدِيُّ قَالَ: شَهِدْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، وَقَالَ مُحَمَّدُ بْنُ عَمْرٍو قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، وَرُبَّمَا قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ فِي الصَّلَاةِ، فَتَرَكَ شَيْئًا لَمْ يَقْرَأْهُ، فَقَالَ لَهُ رَجُلٌ: يَا رَسُولَ اللَّهِ، تَرَكْتَ آيَةَ كَذَا وَكَذَا؟ قَالَ: «فَهَلَّا أَذْكَرْتُمُونِيهَا» . زَادَ مُحَمَّدُ بْنُ يَحْيَى فَقَالَ: كُنْتُ أُرَاهَا نُسِخَتْ

Amesema Muhammad Ibn Yahya kua amesema Al Humaydi kua amesema Muhammad Ibn Amr Ibn Tamam Al Misri kua amesema Yusuf Ibn Adi kua amesema Marwan Ibn Miawwiyah kua amesema Yahya Ibn Kathir Al Kahli kua amesema Miswar Ibn Yazid Al Usayd na Yahya Ibn Al Asadi *Radhi Allahu Anhum* kua:Nimemshuhudia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*

Na Muhammad amesema kua: Ibn Amr amesema kua Nilimsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisoma Qur'an kwenye Sala na hivyo akawacha kitu bila ya kukisoma.'

Hivyo baada ya kumaliza Kusali basi kuna Mtu akasema kumwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:*Ya Rasul Allah* naona hukuisoma Aya kadha wa kadha.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Sasa kwanini hamkunigutua juu yake?'**

Muhammad Ibn Yahya *Radhi Allahu Anhu* akaongezea kwa kusema: 'Kwa sababu nilidhania imebatilishwa.' *(Sahih Ibn Huzaymah)*

Na tunapoiangaliahadithi hii basi tunaona kua ni hadith inayoonesha umuhimu wa kugutuana pale Mtu anapokosea ua anaposahau ndani ya Sala Kiasi ya kua Masahaba *Radhi Allahu Anhum* waliamua kuweka watu maalum kwa ajili ya kuwasimamoa nyuma yao ili wagutuliwe watakapokosea kama tulivyoona katika mfano wa kisa cha Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* tulichoanza nacho.

Ambapo na pia kuna mfano wa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambae anasema kua: '**Masahaba *Radhi Allahu Anhum wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua wakigutuana katika Sala,na baadhi walikua wanapoanza Sala basi humuweka Mtu nyuma yao ili afuatilie Sala zao ili kama wakikosea basi Wakumbushwe.'**

Na hii ni kama alivyosema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Amir Ibn Rabiah amesema kua: Wakati mimi nilipokua katika Mji wa Makkah Safari moja, nilimuona Mtu akiwa anasali katika Maqam Ibrahim, huku kukiwa na Mtu mmoja Nyuma yake ambae alikua akimsaidia Mtu huyo, na nilipomuangalia vizuri Mtu huyo nikaona kua alikua ni Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anh**u.***'*(Al Mughni)*

Na kwa upande mwengine basi anasema Imam Al Bukhari kua:

حَدَّثَنَا آدَمُ حَدَّثَنَا شُعْبَةُ قَالَ: حَدَّثَنَا الأَزْرَقُ بْنُ قَيْسٍ قَالَ: "كُنَّا بِالأَهْوَازِ نُقَاتِلُ الْحُرُورِيَّةَ، فَبَيْنَا أَنَا عَلَى جُرُفِ نَهَرٍ إِذَا رَجُلٌ يُصَلِّي، وَإِذَا لِجَامُ دَابَّتِهِ بِيَدِهِ، فَجَعَلَتِ الدَّابَّةُ تُنَازِعُهُ، وَجَعَلَ يَتْبَعُهَا -قَالَ شُعْبَةُ: هُوَ أَبُو بَرْزَةَ الأَسْلَمِيُّ- فَجَعَلَ رَجُلٌ مِنَ الْخَوَارِجِ يَقُولُ: اللَّهُمَّ افْعَلْ بِهَذَا الشَّيْخِ. فَلَمَّا انْصَرَفَ الشَّيْخُ قَالَ: إِنِّي سَمِعْتُ قَوْلَكُمْ، وَإِنِّي غَزَوْتُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ- سِتَّ غَزَوَاتٍ أَوْ سَبْعَ غَزَوَاتٍ وَثَمَانَ، وَشَهِدْتُ تَيْسِيرَهُ، وَإِنِّي أَنْ كُنْتُ أَنْ أُرَاجِعَ مَعَ دَابَّتِي أَحَبُّ إِلَيَّ مِنْ أَنْ أَدَعَهَا تَرْجِعُ إِلَى مَأْلَفِهَا فَيَشُقَّ عَلَيَّ

Amesema Adam kua amesema Shubah kua amesema Al Azraq Ibn Qays kua: 'Sisi tulikua katika maeneo ya Al Ahwaz(Ambalo leo hii ni eneo la baina ya Iraq na Iran karibu na Mji wa Basra) tukipigana na Watu waliokua wakipingana na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*. Na mimi nilikua kwenye mwambao wa Mto ambapo pembeni yake alikuwepo Mzee Mtu mzima ambae alikua akisali juu ya Farasi wake huku akiwa ameshikilia Hatam za Farasi huyo.

Hivyo Farasi huyo akaanza kuzivuta Hatamu hizo huku na kula huku Mzee huyo akiwa ni mwenye Kuvutwa na na Mvuto huo wa Farasi huyo na yeye akiwa bado anaendelea na Sala yake, bila kuikata Sala hio.

Ambapo anasema Shubah ambae pia ni miongoni mwa walionukuu riwaya hii kua Mzee huyo alikua Sahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliekua akiitwa Abu Barzah Al Aslami *Radhi Allahu Anhu.* Hivyo Mmoja kati ya watu waliokua wakipingana na Ali Ibn Abi *Talib Radhi*

***Allahu Anhu* akasema: 'Mwangalieni huyu Mzee namna anavyoibatilisha Sala yake kwa ajili ya Farasi wake!'**

Na Abu Barzah Al Aslami *Radhi Allahu Anhu* baada ya Sala akasema: 'Kwa hakika mimi nimesikia Mliyokua mkiyasema, na kwa hakika mimi nimefunga Safari na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mara sita au saba au nane(Ambapo Hapa Shu'bah alikua hana uhakika ilikua mara ngapi)

Abu Barzah Al Aslami *Radhi Allahu Anhu* akaendelea kusema kua: 'Hivyo nimeshuhudia namna Mambo yalivyorahisishwa kwa Watu katika Uislam. Na hivyo kwangu mimi ni bora zaidi kua nnatembea upande huu na ule huku nikiwa nnasali Juu ya Farasi wangu, kuliko kumuachia Farasi wangu awe ni mwenye kuenda anakotaka huku mimi nikiwa chini nnasali na kujiingizia Mashakil ya Kufikiria juu ya Farasi wangu ameelekea wapi.'*(Sahih Bukhari)***

Ambapo kuhusiana na Riwaya hii basi tuaona kua kuna tatizo la uhibitisho kwa wale wanaosema kua Abu Barzah Al Aslami *Radhi Allahu Anhu* alifariki mnamo mwaka 64 Al Hijra na hii ni kwa sababu Vita hivi ambavyo ni vita vya Siffini vilipiganwa mnamo mwaka65 Al HIjra.

Na ingawa Wanazuoni wanasema kua tukio Hili lilitokea katika mwambao wa Mto Dujailah lakini baadhi ya Wanazuoni wanasema kua Abu Barzah Al Aslami *Radhi Allahu Anhu* alikua akisali Sala yake hii si kwenye mwambao wa Mto Dujail bali ilikua ni kwenye kivuli cha Ngone inayojulikana kama Ngome ya Mahran ambayo ipo karibu na mwambao wa Mto Dujail.

Abu Barzah Al Aslami *Radhi Allahu Anhu* alikua akisali Sala yake hio katika wakati wa Al Asr, na pia wanasema kua Abu Barzah Al Aslami alifunga Safari na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* mara Saba.

Ambapo kwanza tunapoiangalia Hadith hii basi tunaona kua Mtu anaweza akazungumzia Sifa zake pale itakahitajika lakini si kwa Malengo ya kujiona au Kujisifu. Halafu pia ndani yake Mna Mtizamo wa Fiqh ambao ni wenye kuruhusu Mtu anaesali kua na uhakika wausalama wa Mali yake na Nafsi yake, kwani Jambo la kuhakikisha usalama Mali yake Mtu au Nafsi yake, Familia yake, Uhai wa Ibn Adam mwenzake n.k hua ni Wajibu hata pale mtu huyo anapokua ndani ya Sala.

Hadith hii pia inaonesha kua Abu Barzah Al Aslami *Radhi Allahu Anhu* katika wakati alipokua anasali basi Farasi wake alikua akimvuta huku na kule kunakosababisha kukosekana kwa utulivu wa Kiwiliwili ambako hua kunakubalika katika hali kama hii.

Ambapo hata hivyo hua inatakiwa pia kua Mtu awe ameelekea upande wa Kibla, kwa sababu kama akigeukia katika Upande ambao sio wa Kibla basi Sala yake Ingebatilika, na hivyo itambidi Mtu Husika aisali tena Sala yake Upya. Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: '**Hairuhusiki kwa Mtu Kusali Sala ya Fardhi kwa kuelekea katika Upande usiokua wa Kibla, na hairuhusiki kwa Mtu kufanya hivyo kutokana na kupenda yeye mwenyewe na kuna Makubaliano ya Wanazuoni Juu ya Jambo hili, Isipokua pale Mtu atakapokua katika Hali ya Khofu.'**

Na bila ya shaka ningependa kuifafanua Hadith hii kulingana na Mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kama alivyoeleza katika Fat-h Al Barr na pia kulingana na Mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Muhammad Al Qastallani Al Shafii kama alivyoelezea katika Irshad Sari

Kwa tungeweza kunufaika zaid na kupata raha zaid juu ya ufafanuzi wao Maimamu hawa wawili yaani Al Asqallani na Al Qastallani. Lakini bora wacha tuendelee na Sala juu ya Kipando.Kwani anasema Imam Ahmad Ibn Naqib Al Misri kua:

Kuelekea Upande wa Kibla hua ni Sharti la lazima kwa ajili ya kuifanya Sala ya Mtu husika anaeisali iwe ni yenye kukubalika, kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Isipokua pale itakapokua ni katika Hali ya Hatari, au ni katika Kusali Sala za Sunnah ambazo Mtu atakua anasali wakati akiwa Safarini.

Kwani kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua ni Lazima kuelekea katika Upande sahih wa Kibla kwa kadiri itakavyowezekana.'*(Umdat Salik wa Uddat An Nasik)*

Naam hivyo basi hua inaruhusika Kusali juu au ndani ya Kipando lakini kwa sharti la kua uwe ni mwenye kuelekea upande wa Kibla.

Na kama ikiwa ni Sala ya Sunnah basi hata kama Kipando kikigeukia upande mwengine basi hua hamna tatizo.

Lakini kama ikiwa ni Sala ya Fardhi au Sala ya Maiti basi Kuelekea Kibla hua ni Lazima, kwa mana hio kama umepanda Meli na ukaanza kusali Sala ya Fardhi huku meli hio ikiwa imeelekea Kibla lakini baadae ikabadilisha muelekeo wakati wewe bado umo ndani ya Sala basi katika hali kama hii hua inakubidi wewe mwenyewe ugeuke mzima mzima ndani ya Sala yako na kuelekea Upande Sahih wa Kibla, la sivyo basi Sala yako itakua Batili.Na huo ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua unapokua katika hali kama hii basi sio Lazima kugeuza Mwili Mzima, bali itatosheleza kugeuza Uso tu katika Upande wa Kibla kama kiwiliwili chote haitowezekana.

Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa zamani wa Imam Al Shafii, na hii ni kutokana na Hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua:

قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : مَا بَيْنَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ قِبْلَةٌ

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kile kilichopo baina ya Mashariki na Magharibi ndio Kibla*(Sunan Ibn Majah)*

Ambapo Anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi kua: '**Mtizamo huu ndio pia Mtizamo wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Imam Abd Allah Ibn Mubarak na Imam Abu Hanifa.'***(Al Majmuu)*

Na kwa upande wa Imam Ahmad Al Rifai basi anasema kua: '**Mtizamo huu umenukuliwa na Imam Al Muzani, na kwa sababu Imam Al Muzani ameunukuu Mtizamo huu, basi kuna wasemao kua ni Mtizamo mpya wa Imam Al Shafii, na kwa upande wa Imam Hasan Al Jurri ambae ni muandishi wa Murshid basi nae ameupendelea Mtizamo huu pia.'***(Kifayat Al Nabih)*

Hivyo kama tulivyoona kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Kulichopo baina ya Magharibi na Mashariki ndio Kibla.'***(Sunan Ibn Majah)*

Ambapo hata hivyo Hadith hii haimaanishi kua popote pale alipo akitaka Kusali basi angalie Magharibi ni wapi na Mashariki ni wapi na kisha aamue baina yake ndio afanye Kibla.La Hasha!

Kwani amesema Shaykh Ul Islami Al Hafidh Zayn Ad Din Abd Rahman Al Iraqi Al Qurdi Al Shafii kuhusiana na hadith hii kua: **Hili Si Jambo linalojumuisha maeneo ya Ardhi ya nchi zote, bali hua ni kulingana na Mji Mtakatifu wa Makka na Miji inayolingana na Muelekeo wa Kibla chake n.k** Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Mujaddid Ad Din, Shaykh ul Islami Imam Jalal Ad Din Al Suyuti Al Shafii. Ambao ndio pia Mtizamo wa Imam Abu Bakr Ahmad Al Bayhaqi Al Shafii.

Na amesema Imam Ahamd Ibn Khalawayh Al Rahabi kua: '**Nchi zote zina Latitudo zake kulingana na Kibla, hali hii ya hadithi hio hio hua inatumika kwa upande wa watu wa Kusini na Kaskazini wana Latitude zao.'**

Na Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Abu Umar Al Namari Al Andalus Al Qurtubi Al Maliki amesema kua: '**Tafsiri ya Kauli ya Ahmad Ibn Hanbal kua Hili lipo kwa nchi zote ni kwa ajili ya Watu wao zina Kibla chao Mfano kama Madina Upande wao wa Kibla ni Kusini ambapo ndipo liliopo Al Kaabah, hivyo wanakabiliana nalo, baina ya Magharibi yao na Mashariki yao, ambapo Magharibi hua Kulia kwao na Mashariki hua Kushoto kwao.Ambapo Watu wa Yemen wana latitudo zak kulingana na Kibla kama watu wa Madina isipokua wao wakilielekea Al Kaabah basi Mashariki huiweka Kuliani kwao na Magharibi huiweka Kushoto kwao.**

Watu wa Iraq na Khurasan pia wana Latitudo zao wanapoelekea Kibla isipokua Kwao wao Kibla hua ni baina ya Kaskazini na Kusini na kadhalika kwa waliokuwepo katika Upande unokabiliana na Iraq.Kibla hua ni kidogo kwa watu wa Masjid Al Haram, na ni kipana zaidi kwa watu wa Mji wa Makkah kuliko kwa walioko Masjid Haram, na ni kikubwa zaidi kwa wengine kulingana na tulivyoelezea.'

Kwa Maana hio basi Mtu anapokua anasali Sala ya Sunna Juu ya Kipando Au Ndani ya chombo cha Usafiri kinachosafiri, na kisha chombo hicho kikaelekea Upande ambao sio wa Kibla basi Mtu anaruhusika kuendelea na Sala yake huku akiwa ameelekea Upande ulioelekea Kipando hicho au chombo hicho. Lakini hii kama chombo husika kitakua chembamba, kwa mfano kama Farasi, Mashua, Ndege n.k. Ila kama kitakua kipana na ataweza kukielekea Kibla basi itambidi akielekee Kibla.

Na pia Mtu anapokua katika Hali ya Hatari na hivyo kua na Khofu kubwa juu ya Usalama wake basi anaruhusika kusali bila ya kuelekea Kibla na hivyo Anaruhusika kuelekea upande wowote kulingana na mazingira yake iwe Sala hio ni ya Sunnah au ya Fardhi.

Ama kuhusiana na Sala ya Fardhi na Sala ya Maiti basi Kuelekea Kibla hua ni Wajibu, lakini hata hivyo pale inapokua ni Sala ya Fardhi na Mtu yuko ndani ya Chombo ambacho hawezi kuelekea Kibla ndani yake basi hapa anaruhusika kutoelekea Kibla pia.

Ila kama anaweza kusimamisha Chombo au Mnyama husika ili ashuke kisha aelekee Kibla basi itambidi afanye hivyo na hii ni kwa sababu ya ile hadith isemayo kua:

عَنْ جابر بن عبد الله رضي الله عنهما: "أن النبي صلى الله عليه وسلم كان يصلي على راحلته نحو المشرق، فإذا أراد أن يصلي المكتوبة نزل فاستقبل القبلة

Amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua:'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akisali Juu ya Kupando chake huku akiwa ameelekea upande wa Mashariki. Na alipokua akitaka Kusali Sala ya Fardhi basi alikua ni mwenye kushuka kutoka juu ya kipando chake na kisha huelekea Kibla na Kusali'*(Sahih Bukhari)*

Na akasema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:

عن عبد الله بن عمر رضي الله عنهما «أن رسول الله صلى الله عليه وسلم كان يُسَبِّحُ على ظَهرِ رَاحِلَتِه حَيثُ كان وَجهُهُ، يُومِئُ بِرَأسِهِ، وكَان ابنُ عُمرَ يَفعَلُهُ». وفي رواية: «كان يُوتِرُ على بَعِيرِه». ولمسلم: «غَيرَ أنَّه لا يُصَلِّي عَليهَا المكتُوبَة». وللبخاري: «إلا الفَرَائِض».

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:'***Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam* aliakua akimtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika wakati alipokua Juu ya Kipando chake kuelekea Upande wowote ule.Na alikua akiinamisha na kuinua Kichwa Chake. Na Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua kaifanya hivyo pia.'**

Nakuna Hadith isemayo kua; 'Alikua akisali Salat Al Witr akiwa juu ya Ngamia wake.'

Ambapo kwa upande wa Hadith iliyonukuliwa na Imam Muslim basi inasema kua: Lakini hata hivyo hakuwahi kusali Sala ya Fardhi wakati akiwa juu yake.'

Ambapo kwa upande wa Hadith iliyonukuliwa na Imam Bukhari basi inasema kua: isipokua katika kusali Sala ya Fardhi.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hadith hii ni yenye kudhihirisha Uthibitisho wa kua hairuhusiki kwa Mtu Kusali Sala ya Fardhi bila ya kua ni mwenye kuelekea Kibla**. **Na haikubaliki kufanya hivyo kwa Utashi wake tu na kuna Makubaliano ya Wanazuoni Juu yake isipokua pale Mtu atakapokua katika hali ya Kua na khofu kubwa.'**

Na amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿قَدْ نَرٰى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَآءِۚ فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضٰىهَاۗ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِۗ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوْا وُجُوْهَكُمْ شَطْرَهٗۗ وَاِنَّ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ لَيَعْلَمُوْنَ اَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّهِمْۗ وَمَا اللّٰهُ بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُوْنَ﴾

Qad narâ taqalluba waj-hika fis-samâ', fa lanuwalliyannaka qiblatan tardlâhâ fa walli waj-haka syathral-masjidil-ḥarâm, wa ḥaitsu mâ kuntum fa wallû wujûhakum syathrah, wa innalladzîna ûtul-kitâba laya'lamûna annahul-ḥaqqu mir rabbihim, wa mallâhu bighâfilin 'ammâ ya'malûn. *(Surat Al Baqara 2:144)*

Tafsir: ***Tumekuona ewe Muhammad (Salallahu Alayhi wa Salam)ukiwa ni mwenyekugeuzia Uso wako Juu Mbinguni. Hivyo sasa hivi tunakuelekezea Muelekeo utakaokupendezesha. Hivyo elekezea uso wako katika Masjid Haram(Makkah) popote pale utakapokuwepo elekezea uso wako upande huo.***

Kwa hakika wale waliopewa vitabu (Ahl Al Kitab) ni wenyekuujua ukweli kutoka kwa Mola wao. Na Allah si mwenye kughafilika na wanayoyafanya.

Hivyo aya hii pia ni kithibitisho cha Wajibu wa kuelekea katika Kibla cha Masjid Al Haram katika Ibada ya Sala.**Lakini hapo hapo kwa kua Uislam si Dini yenye kufanya mambo yawe Magumu basi kama tulivyoona kua kuna Hali za Dharura ambazo zinampelekea Mtu anaesali kuruhusika kutoelekea Upande wa Kibla.**

Ambapo Mbali ya kua Hatarini au katika sehemu isiyotosha kwa Mtu anaesali kuelekea Upande wa Kibla lakini pia pale Inapokua Mtu ni mgonjwa na hawezi yeye mwenyewe kuelekea Upande wa Kibla hadi apewe msaada wa kunyanyuliwa, na wa kumnyanyua hayupo kwani yuko peke yake.

Hivyo katika hali kama hii basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad Ibn Hanbal wao wanasema kua:Yeyote yule ambae hawezi kuelekea Kibla, na hakuna wa kumgeuizia upande wa Kibla basi kwake yeye hua anaruhusika kusali kwa kuelekea upande anaoweza kuelekea Na hatotakiwa kuirudia Sala hio hapo baadae.

Na hii ni kwa Sababu Kuelekea Kibla hua kunaruhusika kuachana nako pale inapokua hakuna uwezekano wa kuelekea Kibla. **Ambapo ingawa hii ni kwa Mtizamo wa Imam Abu Hanifa lakini kwa upande Wanafunzi wake ambao ni Imam Al Shaybani na Imam Abu Yusuf wao wanasema kua Sala hio haisihi.**

Na anasema Imam Al Kasani Al Hanafi kua: Kama ikiwa Mtu hawezi kuelekea Kibla mbali ya kua ni mwenye kujua kua upande fulani ndio Kibla, basi anaruhusika kuelekea katika Upande wowote awezao.Kwani amrisho la kuelekea Kibla hua limefutwa kwa Mtu kama huyu kama vile ambavyo lilivyokua limefutwa kwa Mtu mwenye Khofu dhidi ya Maadui zakeHivyo, kama Mtu hawezi na hakuna Mtu wa kumsaidia kuelekea Kibla basi sharti la kuelekea Kibla linafutwa kwake*(Badai Al Sanai)***

Ambapo kwa upande wa Al aAlamah Ibn Maazah Al Hanafi basi nae amesema kua: '**Tofauti baina ya Mtu mwenye Afya na asiekua na Afya yaani Mgonjwa hua si katika yale asiyoyaweza kuyafanya bali hua ni katika yale ambayo anayo uowezo wa kuyafanya, kua kuyafanya kwake ni kama mwenye Afya ama la.**

Hivyo kama anakijua Kibla ni upande gani lakini hawezi kuelekea Kibla na hakuna wa kumsaidia katika kumuelekeza Kibla, basi jawau lake ni kua anaelekea upande anaoweza kuelekea. **Na wala hatowajibika kuirudia Sala hio, kwani yale asiuoyaweza kuyafanya katika Masharti hua hayana nguvu kuliko yale anayoyaweza kuyafanya yanayojumuisha Nguzo za Sala**. **Hivyo kama atapata Mtu wa Kumelekeza Kibla basi na amuombe Mtu huyo amuelekeze Kibla na kama akikosa basi anaruhusika kusali huku ameelekea Upande ambao si wa Kibla.**'(*Al Muhiit Al Burhan Fi Fiqh Al Nuuman)*

Na akasema Imam Ibn Nujayn Al Hanafi kua: '**Na Mtu mwenye Khofu basi hua anaruhusika kuelekea Upande wowote anaweza kuelekea katika Sala yake**. **Kwa sababu kuelekea Kibla hua ni Sharti la Sala ambalo linaruhusika kutotimizwa pale inapokia hakuna uwezekano wa kulitimiza Na Mtu mwenye Khofu hua ana sababu inayokubalika kisharia sambamba na Mgonjwa nae pia ana sababu inahokubalika kisharia pale inapokua hakuna wa kumuelekeza Upande wa Kibla**. **Kwani hii hua ni sawa na Mtu mwenye uwezo wa kufanya kitu kutokana na kuwezeshwa na mtu mwengine kufanya kitu hicho.'** (*Bahr Al Raiq)*

Kwani kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Imam Al Mardawi Al Hanbali kua: '**Ama kuhusiana na Kuelekea Upande wa Kibla basi hua ni Wajib ila inapotokea haki ya kutokuwepo uwezekako huo kwa mfano kam kumetokea Vita, au kwa Mtu mwenye kuumwa na hivyo hawezi kuelekea Kibla na hakuna Myu wa kumsaidia kuelekea Kibla basi hua inaruhusika Kuelekea Upande mwengine wowote, na huo ndio Mtizamo sahih zaidi katima Madhhab yetu.'***(Al Ansaaf)*

Na akasema Imam Al Hajjawi Al Hanbali kua: '**Kuelekea Kibla hua ni sharti la Nane la kukubalika kwa SalaHivyo Sala hua ni batili pale inaposaliwa bila ya Kuelekea KiblaIsipokua kwa yule mwenye Udhuru hata kama utakua ni wa kipekeeKwa mfano Mtu anapokua mgonjwa na hawezi kuelekea Kibla, au hana mtu wa kumuelekeza, au Labda Mtu huyo ni mfungwa na amefungwa Kamba n.k, basi katika hali kama hii hua inaruhusika kwa mtu husika kuelekea upande anaoweza kuelekea katika Sala yake hata kama utakua si upande wa Kibla, na haitomhitajia Mtu huyo kuirudia Sala hio.'***(Al Iqna)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malika basi amesema Imam Al hattab Al Maliki kua: '**Amesema Ibn Bashir kuhusiana na Sala ya Mtu anaeumwa kua:**'**Kama itakua Mtu hawezi kuelekea Kibla yeye mwenyewe basi itabidi asaidiwe kuelekezwa Kibla, na kam hakuna uwezekano huo basi Sharti la kuelekea Kibla hua halihusiani nae Mtu husika yaani hua saaa na Mtu aliekua katika Mpigano ya vita**. **Na akisali katika hali hio ya kutoelekea Kibla katika wakati huo basiItambidi Sala hio airudie tena pale atakapopata Afya yake.'***(Mawahib Al Jalil Li Sharh Mukhtasar Al Khalil)*

Na akasema Imam Asbagh Al Maliki kua: '**Kama ikiwa mtu atakua hawezi kuelekea Kibla na hakuna wa kumsaidia kukielekea Kibla, basi atasali kuelekea katika Upande atakaoweza kuelekea, na itambidi airudie Sala hio pale atakapokua katika hali ya kua ni mwenye kuweza kuelekea Kibla.'**(*Al Wadiha)*

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam al Shafii basi anasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Diin Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kwa Mtu asieweza kuelekea Kibla yeye mwenyewe, na asiepata Mtu wa Kumuelekeza, iwe kwa malipo au bila ya malipo basi humbidi kusali kwa kuelekea Upande atakaoweza kuelekea kulingana na hali yake, na kisha atakapopata nafasi ya kua ni mwenye kuweza kuelekea Kibla mwenyewe basi atarudia Kusali Upya Sala hizo**.'*(Al Majmuu)*

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَلِلَّهِ ٱلْمَشْرِقُ وَٱلْمَغْرِبُ ۚ فَأَيْنَمَا تُوَلُّواْ فَثَمَّ وَجْهُ ٱللَّهِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ﴾

Walillahi almashriqu waalmaghribu faaynama tuwalloo fathamma wajhu Allahi inna Allaha wasiAAun AAaleemun*(Surat Al Baqara 2:115)*

Tafsir: ***Kwa Allah ndiko Kwenye Umiliki wa Mashariki na MagharibiHivyo Kokote kule MtakakoelekeaBasi Kuna Muonekano wa AllahKwa Hakika Allah ni mwenye kutosheleza Kwa Waja wake na ni mwenye kujua juu ya kila Kitu****.*

Ambapo ingawa aya hii ni yenye kuzungumzia kuhusiana na Kibla, na ilishushwa kwa ajili ya kuwajibu watu wa Ahl Al Kitab kuhusiana na Hoja yao juu ya kwanini Kibla kikabadilishwa kutoka Bayt Al Maqdis na kuelekeza katika Mji wa Makkah.

Lakini anasema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu k*uhusiana na Sababu ya kushushwa kwa aya hii kua: '**Aya hii imeshushwa kwa ajili ya Sala za Sunna Na hivyo Wanazuoni wengi ni wenye kusema kua aya hii ndio iliyotoa ruhusa kusali juu ya Kipando.'**

Na pia Wanazuoni wanakubaliana kua inaruhusika Kusali Juu ya kipando katika Safari zote.Isipokua kwa Upande wa Imam Malik basi yeye anasema kua kwa sharti la kua Masafa ya Safari yawe ni sawa na masafa yanayoruhusiwa Mtu kufupisha Sala.Ambapo habari ya Sala ya Safari tutazungumzia baadae katika Mlango wake Inshaa Allah.

Na Wanazuoni wanakubaliana pia kua **Hairuhusiki kwa Mtu Kusali Sala ya Fardhi juu ya Kipando isipokua pale itakapokua kua Sababu inayokubalika Kisharia.**

Ingawa hata hivyo, kama ikiwa Mtu atasali Sala ya Fardhi juu ya kipando na akawa ni mwenye Kutimiza Masharti yote ya Sala na Nguzo zote za Sala, basi Sala yake hua inakubalika. Na hii ni kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik, Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal Japokua katika hili basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Hanbal hawakuweka Sharti la kua Kipando hicho kiwe ni kilichotulia katika sehemu moja au ni chenye kutembea.

Lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wamesema kua kwa Sharti la kua Kipando hicho hata kama ikiwa cha usafiri basi iwe Kimetulia. Kwani kikiwa kinatembea basi hua hairuhusiki kwa sababu ya Mwendo ni wenye kunasibishwa nacho.

Na Pia hata hivyo Wanazuoni wameruhusu kwa Mtu Kusali Sala ya Fardhi katika Kipando kwa sababu zifuatazo: '**Pale mtu anapokua na Khofu ya Uhai wake au Mali zake kutokana na hatari ya Maadui au Wanyama wa hatari, kutokana na Khofu ya kukimbiwa na Msafara wa wasafiri, kutokana na Khofu ya kupata madhara yatakayotokea katika wakati wa Mvua, Tope, Theluji n.k.'**

Lakini kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hua ni lazima kuzirudia Sala hizo Hivyo kwa Mtu anaesafiri kwenye Basi,Meli, Ndege, Treni n.k hua ana hali hiari ya kuchagua moja kati ya njie zifuatazo katika kutekeleza Ibada ya Sala ya Fardhi katika Safari yake ambazo ni;

1-Asali huku akiwa amesimama huku akiwa ameelekea Kibla Ndani ya Chombo Husika wakati akiwa Safarini na kutimiza nguzo zote za Sala. **Lakini chombo kiwe kimetulia isiwe kinaelekea huku na kule, ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Hanbal hua hamna tatizo Hususan pale inapokua Mtu huwezi kukisimamisha chombo husika.**

2-Kama haiwezekani kusimama kwa kukosekana nafasi labda tuseme, basi Mtu akae Kitako katika Kusali Sala yake hio ya Fardhi, na hivyo atakua si mwenye kuweza kusimamisha nguzo zote za Sala lakini kwa kua hana chaguo jengine isipokua kukaa basi itambidi asali huku akiwa amekaa kitako.

Na kama ni kipindi cha Sala ambayo anaweza kuchanganya Sala basi na Achanganye, yaani Dhuhr na Al Asr na Maghrib na Isha, kama kwa kuitanguliza Sala, au kuiwahisha na kama haiwezekani Kuchanganya Sala basi asichanganye. Hivyo kama Safari itakua ndani ya Nyakati za Sala mbili basi ataruhusika kuzisali Sala zote hizo ndani ya Chombo hicho cha Usafiri.

Na pia itakua ni vizuri zaid kama ikiwa Baada ya kufika Mtu kuwasili akasali upya Sala hizo kama ataweza kwa kuzirudia kama kawaida, ambapo hii itasaidia kuondoa Tofauti ya Kimtizamo kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Na anasema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:

سُئِل النبي صلى الله عليه وسلم : كيفَ أصلي في السفينةِ ؟ قال : صَلِّ فِيهَا قَائِمًا إِلَّا أَنْ تَخَافَ الْغَرَقَ

'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa kuhusiana na Kusali kwenye Meli?'**

Ambapo nae akasema: 'Sali huku ukiwa Umesimama isipokua pale utakapokua na Khofu ya Kuzama' *(Imam Ad Daraqutni, Imam Al Bayhaqi Maarifat Al Sunnan wa Al Athar)*

Na pia anasema Imam Ibn Abi Shaybah kua:

قال عبد الله بن أبي عتبة مولى أنس رضى الله عنهما: "سافرت مع أبي سعيد الخدري وأبي الدرداء وجابر بن عبد الله رضى الله عنهم جميعًا، فَكَانَ إِمَامُنَا يُصَلِّي بِنَا فِي السَّفِينَةِ قَائِمًا، وَنَحْنُ نُصَلِّي خَلْفَهُ قِيَامًا، وَلَوْ شِئْنَا لَأَرْفَأنَا وَخَرَجْنَا" رواه ابن أبي شيبة

Amesema Abd Allah Ubn Abi Utbah ambae ni Mtumwa aliachwa huru na Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu* kua: Mimi nilisafiri pamoja na Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu,* naAbu Al Dardaa *Radhi Allahu Anh*u na Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu*.Ambapo Imamu wetu alituongoza Sisi kwenye Sala huku tukiwa tumesimama ndani ya Meli Tulikua tukisimama Nyuma yake, na kama tungetaka basi tungeondoka na kuchana nae.'*(Musanaf Imam Ibn Abi Shaybah)*

Hivyo anasema Imam Al Kasani Al Hanafi kua: '**Inaruhusika Kusali Juu ya Mnyama, iwe Mnyama huyo anaweza kuliwa ama la.'***(Badai Al Sanai)*

Na akasema tena Imam Al Kasani kua: **'Inaruhusika Kusali ndani ya Meli, hata kama ikiwa ni vigumu kusimama ndani yake**. **Na hii ni kwa sababu Kusali kwenye Meli hua ni sawa na kusali juu ya Ardhi, kwani kutotulia kwake hua hakutokani na Meli yenyewe ambako hakuendani na Sala bali kunatokana na Mawimbi ya Bahari yenyewe na hivyo hua ni tofauti na kutotulia kwa Mnyama.'***(Badai Sanai)*

Na akasema Imam Ali Shurunbulali Al Hanafi kua**: 'Kusali Sala ya Fardhi kwenye Meli wakati ikiwa inaenda huku anaesali akiwa amekaa Kitako hua Kunaruhusika na ni Sahih kulingana na Mtizamo Wa Imam Abu Hanifa.'***(Maraqi Al Falah)*

Ambapo kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi anasema Imam Alish Al Maliki kua: '**Kama ikiwa Sala itaanza katika wakati ambao Meli itakua imeelekea Kibla na kisha ikageukia upande ambao sio wa Kibla basi kama kuna uwezekano kwa yule anaesali kuelekea Kibla atageukia Upande wa Kibla na kama ikiwa hakuna uwezekano basi Mtu huyo ataelekea Upande anaoweza kuelekea, na hakuna tofauti juu ya hilo Iwe kwa Sala ya Sunnah au ya Fardh***i.'(Manhaj Al Jalil)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf kua: '**Sala ya Fardhi hua inakubalika ndani ya Meli, iwe Meli hio imetia Nanga Bandarini au iko Safarini Baharini.**'*(Al Rawdah Talibin)*

Na kwa upande wa Imam Al Husayn Al Hasan Al Shafii basi yeye amesema kua: '**Inakubalika Kusali ndani ya Melo inayosafiri Baharini, tofauti na juu ya Mnyama**. **Kwa Sababu unapokua ndani ya Meli Baharini na Mda wa Kusali Sala ya Fardhi Unapowadia basi inakua haiwezekani kushuka Ardhini kwa ajili ya Kusali, ambapo kwa upande wa Mnyama hua unaweza kufanya hivyo**. **Na kama Mtu ikiwa anakhofu kua akishuka kutoka Juu ya Mnyama wake kwa ajili ya kusali basi atakimbiwa na Msafara, au labda Atadhurika au atapoteza Mali, basi Mtu kama huyu hua anaruhusiwa kusali juu ya Mnyama wake huyo'***(Kifayat Al Akhyar)***

Na akasema Imam Al Imran Al Shafii kua: **'Inaruhusika kusali Sala ya Fardhi ndani ya Meli,iwe meli hio Iko Safarini Baharini au imetka Nanga Bandarini**. **Ama kuhusiana na Wajibu wa Kusimama katika Sala wakati ukiwa ndani ya Meli, basi kama ikiwa Mtu hakhofii Kuhisi, kizunguzungu au kuanguka Baharini katika wakati wa kusimama basi ni Wajib asimame**. **Lakini kama ana khofu hio basi hua hana Wajibu kusimama,na uthibitisho wetu ni Hadith ya Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* aliposema kuan*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwambia Jafar Ibn Abi Talib Radhi Allahu pale alipomtuma Abissiniya baada ya kuulizwa: 'Ya Rasul Allah, Jee nitasalije ndani ya Meli?.'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Sali huku ukiwa Umesimama, isipokua pale utakapokhofia Kutumbukia Baharin**i.''*(Al Bayan)*

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Inaruhusika Kusali Juu ya Mnyama pale inapokua Aliepanda Mnyama anapokua anaumwa na hivyo ni vigumu kwake kupanda na kushuka ambako ni kuzito kuliko inapokua kuna Mvua na Matope na huu ni Mtizamo wa Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu*.'***(Al Kafi)***

Na akasema Imam Al Hajawi Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Inaruhusika Kusali ndani ya Meli kwa Sala zote sio za Sunnah tu huku Mtu akiwa ameelekea Kibla.'***(Al Iqna)*

Naam tunamalizia na Fatwa ya Mufti Ali Jumaa Al Masri Al Shafii ambae anasema kua: '**Kama Mtu anataka kusali ndani ya Ndege basi na asali Sala ya Sunna ndani yake Au asisali kabisa ndani yake.Na hii ni kwa sababu kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii tunaona kua Wanazuoni wanamithilisha sehemu ya Ardhi na sehemu ya Bahari, na wala hawamithilishi sehemu ya Hewa na Bahari.Hivyo kama Mtu akiwa atasafiri kwenye Kitu kinachoelea Angani basi hua hairuhusiwi kwake Kusali kwa Sababu Maumbile ya Hewa hua ni kitu kisichogusika tofauti na yalivyo maumbile ya Maji.**

Wakati Sharti la Wajibu la Sala hua ni kua Kitu kinachosimamiwa juu yake, kinachokaliwa juu yake kinachosujudiwa juu yake katika wakati wa Sala kiwe Kimeshikamana na Ardhi au kimeshikamana na kitu kinachomalizia na kugusana na Ardhi. **Na Safari za Ndege hapa Duniani hua hazizidi masaa 20, kwani husafiri kwa masaa 16 tu na kisha inabidi itue Ardhini.**

Hivyo Kama Ndege itaruka na kisha Itaripuka Angani na Waliokuwemo ndani yake hawajasali basi hua hakuna Jukumu juu yao kwa sababu Wamefariki huku wakiwa si wenye Kudharau Sala na hakuna atakaeweza kuwalipia Sala zao. **Ila inaruhusika kuwalipia Hija na Funga.**

Hivyo Kama Mtu akifariki angani, basi hairuhusiki kumlipia na hii ni kwa sababu Mtu huyo hakudharau Sala yake wala hakuiwacha kwa uvivu,bali aliiwacha kwa sababu ya Kua haiwezekani Kutimiza Masharti ya kukubalika kusali Sala Husika.'

Na bila ya shaka ingawa Mtizamo huu uko sahih lakini huu ni Mtizamo ambao unaweza kuwachanganya wengi miongoni mwa baadhi ya watu. Kwani ni wenye kuingia akilini na kufahamika pale unapokua unatumia Ilm al Mantiq.Na hii ni kwa sababu masharti ya Ibada ya Sala basi ni kua Mtu anaesali anatakiwa awe ni mwenye kusimama, kukaa na kusujudu huku akiwa juu ya Ardhi, au juu ya kitu kilichokua juu ya ardhi au kilichosimama na kitu kilichogusana na Ardhi.

Kwa maana hio basi mtu anapokua ndani ya Ndege hua ni mtu ambae yuko hewani na yuko ndani ya chombo ambacho pia kinaelea juu hewani, hivyo sharti linalohusiana na uhusiaano wa Mtu anaeasali na ardhi hua haliwezi kutekelezeka.

Na nimeainisha Mtizamo huu makusudi ili tupate kujua kuhusiana na Mitizamo tofauti, ili tukija kuona au kusikia mitizamo myengine tusije tukashangaa au tukaona vioja au tukaona kua hivyo Kinyume na maamrisho na kisha watu wakakimbilia kufanya Takfir..yaani kuitana Makafiri jambo ambalo halifai.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Mtu yeyote yule atakaemtoa Muislam mwenzake kwenye Uislam basi Mtu huyo hua ni mwenye kujitoa yeye kwanza kwenye Uislam kabla ya kumtoa mwenzake huyo.'**

Hivyo amesema Imam Al Muzani ambae ni Mwanafunzi wa Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Majukumu ya Kidini hua yanatakiwa kutekelezwa kulingana hali ya Jitihada za mwisho za kiubora kwa Mtu husika. Hivyo hata kama baadhi ya Masharti yakawa hayakutekelezeka kutokana na hali ya ugumu wa mazingira husika, basi Majukumu hayo hukubalika mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hayatohitajia kurudiwa kufanywa tena badala yake.'**

Kwa maana hio basi kuna Mtizamo usemao kua inaruhusika kusali ndani ya Ndege na na hii ni kulingana mtizamo wa baadhi ya Wanazuoni wakiwemo wa Kisalafi.

Sasa tunarudi kwenye ufafanuzi wa Fatwa aliyotoa Mufti Al Jumaa Al Misri Al Shafii ambao ndio mtizamo unaotegemewa na na kukubalika zaidi na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Na moja kwa moja tunamkamata Shaykh Ul Islami Al Aalamah Imam Zakarriyah Al Ansari Al Shafii ambae anasema kua: '***Istiqrar*,(Kusimama kwa umadhubuti juu ya Ardhi) *Wa Al Istqbal*(Kuelekea Kibla) wa *Tamaam Al Arkan* na (Kukamilisha Nguzo za Sala) hua ni Masharti ya kukubalika kwa Sala ya Fardhi.'***(Asna Al-Matalib Sharh Rawd Al-Talib)*. Na huo ndio pia Mtizamo wa Imam Ibn Al Muqri Al Shafii katika Rawdha Talib.

Ambapo Imam Shihab Ad Din Al Ramli Al Shafii akafafanua kauli hii kwa kusema kua: **'Al Istiqrar hua inamaanisha Kusimama au kukaa kwa Uthabiti Juu ya Ardhi katika wakati wa Sala ya Fardhi**. **Hivyo Kama ikiwa Mtu atakua Juu ya Kipando kinachotembea, au yumo Juu ya Kijumba kinachobebwa juu ya Mgongo wa Ngamia, au kama Mtu akiwa amebebwa Juu ya Kitu na Watu na anaelea juu hewani basi Sala yake ya Fardhi itakua ni Batili.'***(Hashiyat al-ramli 'ala asna al-matalib sharh rawd al-talib)*

Ambapo huu ndio pia Mtizamo wa Habib Zayn Ibn Sumayt Al Hadhrami Al Shafii. Hivyo kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii basi kama Mtu utasali Sala ya Fardhi ndani ya Ndege, basi ukitua ardhini katika sehemu unayoenda itakubidi Usali kwa kuirudia tena Sala hio.

YALIYORUHUSIKA NDANI YA SALA KATIKA WAKATI WA KHOFU.

❖❖❖❖

Kwani anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an Tukufu kua:

﴿ حَافِظُوا عَلَى الصَّلَوَاتِ وَالصَّلَاةِ الْوُسْطَىٰ وَقُومُوا لِلَّهِ قَانِتِينَ ۞ فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ فَإِذَا أَمِنتُمْ فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴾

Hafi*dh*oo AAala alssalawati waalssalati alwusta waqoomoo lillahi qaniteena, Fa-in khiftum farijalan aw rukbanan fa-idha amintum faodhkuroo Allaha kama AAallamakum ma lam takoonoo taAAlamoona*(Surat Al Baqara 2:238-239)*

Tafsir: ***Hifadhini Sala ZenuHususan Sala ya Kati na Kati(Al Asr)Na Simameni Mbele ya Allah kwa Unyenyekevu Lakini Kama Mkiwa na KhofuSalini mkiwa mmesimama Kwa Miguu au kwa Juu ya KipandoNa Hivyo Pale Mtakapokua Salama Basi Mkumbukeni Allah Katika SalaKama MlivyofundishwaAmbavyo Mlikua hamjui Hapo Kabla.***

Naam..tumeangalia kuhusiana na akuruhusika Kusali katika hali tofauti kulingana na Mazingira husika, lakini hata hivyo kuna mazingira ambayo bado hatujayaangalia, ikiwemo hili la Juu ya yale yanayoruhusika katika Sala katika wakati ambapo Mtu anakua yuko katika Mazingira ya Khofu ya kukhofia Uhai wake kutokana na Maadui zake, Au mambo yanayohatariaha Maisha.

Na kama tunavyoona Amrisho la aya hii tuliyoannza nayo ambayo ni yenye kutuhimiza kaa kutuamrisha Kuhifadhi Sala, kwa kuzisali ndani ya Nyakati zake na kwa unyenyekevu.Lakini hata hivyo katika Maisha ya Uhai wa Duniani hua kuna mitihani tofauti na kutokana na kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndie Muumba wa Kila kitu na ni mwenye kujua kila kitu yaliyotokea kabla ya Kutokea kwake na baada ya kutokea kwake kulingana na Makadirio yake na Hikma zake, basi ni mwenye kujua kua kutokana na udhaifu wetu kuna baadhi ya wakati haitowezekana kusali kwa Wakati na kwa Utulivu pia.

Na hivyo wakati wa Sala unaweza ukampita mtu na hivyo kuchelewa huko hupelekea kukosekana utulivu ndani ya Sala.Na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta'ala* akahimiza ndani ya Aya hii umuhimu wa Kuhifadhi Sala kwa kuzisali kwa wakati zaidi, ambako kutapelekea kuzisali kwa Utulivu zaidi.Na pia *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kutoa amrisho hili basi akawa ni mwenye kuzipachika Aya hizi katikati baina ya Mada zisizohusiana na Sala kabisa.

Kwani Aya hizi zimepachikwa na kupangwa katika sehemu ya Sura ambayo ni yenye kuzungumzia Mada zinazohusiana na Ufafanuzi wa Hukmu na Miongozo ya Hakiza Wanawake katika mambo yanayohusu Ndoa, Talaka na Ujane.Na hivyo mchomeko huu kwa wasiotafakkari basi huenda wakaona kua umekaa si katika mahala pake.

Lakini mwa wenye Kutafakkari basi watakua ni wenye kuona wazi kua mpangilio huu ni wenye kutudhihirishia umuhimu wa kutosahau Kusimamia na kuhifadhi Ibada ya Sala.Na hivyo hata iwe tupo katika Hali gani au mazingira ya gani basi, ukifika wakati wa Sala tuachane na Kila Kitu kwa ajili ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ndie Muumba wetu na Ndie Muumba wa Kila kitu.Kwani Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndio Malengo ya Kuumbwa kwetu.

Na kutokana na kua hayo ndio Malengo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameamua kutuwekea Muongozo ambao utatupelekea sisi kua ni wenye kujua nini cha kufanya pale itakapokua wakati wa Sala umeingia na sisi tuko katika hali ya kutoweza Kujidhibiti kutokana na kujawa na Hisia za Khofu kulingana na Matukio na mazingira husika.Hisia za Khofu ni Hisia ambazo tumejaaliwa kua nazo kimaumbile kwa ajili ya Kukimbia na Kujiepusha na Madhara na Hatari.

Kwa sababu Sala ndio ndio Ibada inayomjaza Ibn Adam hisia za Khofu ya Mola wake, na hivyo kumuondolea Ibn Adam hali ya Kujihisi kua yeye Mtukufu na Msafi alietahirika kutokana na kasoro na udhaifu wake.Na hivyo Sala kua ni yenye kumrudisha Ibn Adam katika Utiifu wa maamrisho ya Mola wake.Hivyo bila ya Ibada ya Sala basi Ibn Adam asingekua ni mwenye kusimamia Maamrisho ya Mola wake, na hivyo kumuingiza katika hali ya Maangamizo.

Kwani anasema Mujaddid Ad Din, Shaykh Ul Islami, Sultan Al Mutakallimin, Imam Al Mushaqqiqin Imam Al Ghazali Al Thani Imam, Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Al Husayn Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kua:**'Wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* anatuamrisha Kuzihifadhi Sala zetu basi ametumia neno ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua ni Lenye Kumaanisha pande za aina Mbili katika Utekelezaji wa Jambo.**

Kwa mfano tunapoangalia neno Qatala - Kuua - Hua Linamaanisha Kitendo kilichofanyika baina ya pande mbili ambazo ni Mtu alieua na Mtu alieuliwa. Kwa Maana hio basi Neno *Hafadha* linamaanisha kua Kitendo cha Kuhifadhi hapa hua kinasimamiwa na Kutekelezwa na Pande mbili tofauti.

Ambapo pande ya kwanza ni Upande wa Muislam, na jee Upande wa pili ni wa nani?hivyo katika Upande wa pili basi kuna uwezekano wa kufafanua katika hali mbili, ambazo kwa ni kwa upande wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* Ambae ndie anaemlinda Mja wake anaejitolea katika Ibada ya Sala ya kumuabudu yeye kwa kumhifadhi kutokana na Maafa na Matatizo mbali mbali, huku Mtu mwenyewe akiwa ni mwenye Kuihifadhi Sala yake hio.

Na kwa upande wa mwengine basi tunaweza kufafanua kua Sala ndio Yenye Kumlinda na Kumhifadhi Mtu kutokana na Maovu na Maangamizo yule anaeisimamia na Kuihifadhi.' *(Mafatih Al Ghayb)*

Kwani mbali ya kua aya zetu mbili za Surat Al Baqara 2:248-239 ni zenye kuhimiza Kusizisimamia Sala zetu ambazo nazo zitatusimamia katika Maisha yetu hapa Duniani, Kaburini na pia Katika Siku ya Malipo lakini pia: '**Aya zinatuonesha kuruhusika Kusali juu ya Ardhi kwa kusimama, kwa kua juu ya vipando na vyombo na pia kwa kuashiria pale itakapobidi Lakini hata hivyo Kuifupisha Sala katika Rakaa 1, hua ni katika Sala ya Jamaa tu kama ilivyothibitishwa kwenye Qur'an na Sunna.'** *(Tafsir Imam Ibn Jarir)*

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Wanazuoni wengi ni wenye Mtizamo wa kua Sala katika Hali ya Khofu hua ni yenye kuruhusika kufupishwa kwa Rakaa 2 na wala sio 1.'***(Mafatih Al Ghayb)*

Na hivyo basi zinatudhihirishia kuruhusika Kufupisha Sala pale Mtu anapojikuta katika Hali ya Kua na khofu.

Ambapo kwa upande wa Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Imam Hasan Al Basr, Imam Sufyan Ath Thawry na wengineo basi wanasema kua: '**Kama Ikibidi basi Sala hua Inaruhusika**

Kufupishwa inapokua kuna Mazingira ya hali ya Khofu, ambapo Sala ya Rakaa 4 hua inakua ni ya Rakaa 2 katika Safari na inakua ni ya Rakaa 1 katika Hali ya Khofu.'

Ambapo anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Bakr Al Ansari Al Qurtubi Al Maliki kua kuhusiana na aya mbili hizi kua: '**Wakati *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameamrisha kusimama mbele yake kwa Unyenyekevu na Utulivu wa Mwili na Akili katika wakati wa Usalama na Amani.**

Basi pia ameainisha Hali ya Ghafla katika Mazingira ya Khofu pale inapokosekana Amani na Utulivu kwa kudhihirisha kua Jukumu la Ibada ya Sala hua halimuondokei Muuminin kwa hali yeyote ile itakavyokua, na hivyo Amewaamrisha Waumini Ibada ya Sala iwe wanapokua Safarini kwa miguu au kwa kipando cha Farasi, Ngamia n.k, kwa kuashiria kwa Kichwa na viungo vya mwili kokote kule utakapoelekea.

Na haya ndio maneno ya Wanazuoni yanayohusu Sala ya Mtu mmoja mmoja ambae ni mwenye kua na khofu kaama katika Mapigano ya Upanga, au katika Kukimbia Mnyama Mkali Sana anaekufukuzia Au katika Kumkimbia Adui Yako anarkufukuzia, au Katika Mafuriko n.k.

Hivyo aya hizi zinahusiana na kila Jambo ambalo litamtia Mtu khofu Kubwa kwenye Nafsi yake basi ndani yake hua inaruhusika Kufupisha Sala kulingana na Aya hizi. Na Wanazuoni wanakubaliana kua Mtu hua anaruhusika Kufupisha Sala katika hali ya Khofu ambayo inahatarisha Maisha yake kulingana na hali ya mazingira aliyojikuta yake. Na hivyo kua ni mwenye Kuhitajia Kujiokoa Nafsi yake kutokana na hatari hio.

Ambapo anasema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: Hali ya mazingira inayokubalika kwa Mtu mwenye Khofu kusali kwa Kusimama, au Juu ya Kipando, kwa kuelekea Kibla au Bila ya Kuelekea Kibla hua ni katika Mazingira ya Shidat Al Khawf yaani Katika Khofu kubwa sana Ama kuhusiana na Sala ya Khofu ambayo ni Sala ya Jamaa katika wakati wa Vita basi hio hua ni Sala nyengine, na haihusiani na Aya hii, kwani ufafanuzi wake Sala hio ni katika Tafsir ya Surat An Nisaa.'*(Tafsir Al Qurtubi - Jamii Al Ahkami)***

Kwani amesema Imam Al Bukhari kua:

وقال الوليد ذكرت للأوزاعي صلاة شرحبيل بن السمط وأصحابه على ظهر الدابة فقال كذلك الأمر عندنا إذا تخوف الفوت واحتج الوليد بقول النبي صلى الله عليه وسلم لا يصلين أحد العصر إلا في بني قريظة

Amesema Al Walid kua Mimi nilimuelezea Al Awzai kuhusiana na Sala ya Shurahbil Ibn Al Samit na wenzake huku wakiwa juu ya Farasi. Hivyo nae akasema: 'Hivyo Ndivyo iliyokua kwa upande wetu pale tulipokua na khofu ya Kuikosa Sala.'

Na kisha Al Walid akanukuu kama Ushahidi kuhusiana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* pale aliposema kua:Asisali Mtu Sala ya Al Asr isipokua Kwa Banu Qurayza.'*(Sahih Imam Al Bukhari Mlango wa Sala ya Mtu anaewatafuta Wenzake na anaetafutwa huku akiwa Juu ya Kipando)*

Ambapo amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alituelezea kuhusiana na Sala ya Khofu na kisha akasema:Kama Mtu akiwa na Khofu Kubwa sana basi anaruhusika Kusali Ardhini au Juu ya Kipando.'***(Imam Ibn Majah)*

Ambapo Hadith hii imenukuliwa na Imam Al Shawqani katika Kuitafsiri Aya ya 238-239 tulizozingalia hapo kabla.

Na pia imenukuliwa na Imam Malik ambae amesema kua Amesema Imam Nafii kua: '**Sikuona Mimi Abd Allah Ibn Umar kua ni mwenye kuinukuu Hadith hii isipokua ni kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'****(Sahih Muslim, Sahih Ibn Khuzayma, Sunan Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani kua: **'Kuna mitizamo tofauti kuhusiana na maneno yasemayo: 'Kama Khofu ikiwa kubwa zaid basi' kua haya ni maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* au ni maneno ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu?***Ambapo ukweli ni kua hii ni kauli ya*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam'****(Fat-h Al Barr)***

Ambapo kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Hii ni Hadith yenye kubeba Hukmu za Sala ya Khofu, na wala si yenye kutafsiri Aya.'***(Al Majmuu)*

Na anasema Abd Allah Ibn Unays *Radhi Allahu Anhu* kua:

{بعثني رسول الله صلى الله عليه وسلم إلى خالد بن سفيان الهذلي وكان نحو عرفة وعرفات، فقال: اذهب فاقتله، قال: فرأيته وقد حضرت صلاة العصر فقلت: إني لأخاف أن يكون بيني وبينه ما يؤخر الصلاة، فانطلقت أمشي وأنا أصلي أومئ إيماء نحوه، فلما دنوت منه قال لي: من أنت؟ قلت: رجل من العرب بلغني أنك تجمع لهذا الرجل فجئتك في ذلك، فقال: إني لفي ذلك، فمشيت معه ساعة، حتى إذا أمكنني علوته بسيفي حتى برد}

'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **aliniita mimi na kuniambia kua:Nimepata habari kua Khalid Ibn Sufyan Ibn Nubayh Al Hadhali anakusanya Jeshi ili kuniua.Hivyo nenda yuko katika maeneo ya Nakhlah Au Uranah kamuue**. **Hivyo nikaenda na kumkuta Khalid Ibn Sufyan Al Khadhali Baina ya Uranah na Arafat na nilipomuona ilikua tayari ni wakati wa Salat Al Asr.**

Hivyo nikawa na khofu kua kama nikiamua kupigana nae basi nitachelewa katika Sala yangu. **Hivyo nikatembea kumuelekea yeye huku nikiwa nnasali kwa kuashiria**. **Na nilipomkaribia akaniuliza kwa kusema: Wewe ni Nani?**

Nami nikajibu kka kusema: 'Ni Mtu miongoni mwa Waarabu, na nimesikia kua mnakusanya Jeshi kwa ajili ya Kumuua Muhammad.Hivyo nimekuja kujumuika nanyi.'

Ambapo nae akasema: '**Naam Nafanya matayarisho hayo.'**

Abd Allah Ibn Unays *Radhi Allahu Anhu* anaendelea kusema kua Hivyo nikafuatana nae kwa kutembea kwa mda kidogo na kisha nilipopata Nafasi Nikamzidi Nguvu kwa Upanga wangu hadi alipokua Barid*i'(**Sunan Abu Daud, Tarikh Imam At Tabari, Zad Al Maad, Rahiq Al Makhtum)***

Ambapo amesema Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Isami Al Hafidh Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Amesema Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri kua Kila Mwanazuoni ambae nimesoma kutoka kwake ni mwenye kusema kùa:Mtu anaetafutwa na Maadui zake Anaruhusika Kusali Juu ya Kipando chake kwa kuashiria, na kama atakua ni Mtafutaji wa Maadui zake basi Atasali Ardhini.'**

Na akasema Mujaddid Ad Din Mujtahid Al Imam, Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Kama Mtu atakua ametengana na Wenzake na hivyo kua na Khofu kua Maadui zake wanaomtafuta Watamrudia basi anaruhusika kusali juu ya Kipando chake na hii itamtosheleza.Na hili liko wazi kwa sababu kuna utofauti baina ya Mtafutaji Maadui zake na anaetafutwa na Maadui zake kwani Mwenye Kutafutwa na maadui zake hua na Khofu kubwa Zaidi.**

Kwa sababu anaetafutwa hua na Khofu ya Kukamatwa na Maadui zake na anaetafuta hua hana Khofu ya kukamatwa na Maadui Zake bali hua na khofu ya kua Maadui zake watampotea mbele ya Macho yake.'*(Fat-h Al Barr, Al Wajiz Fi Ahkam Al Asir Al Muslim - Utambulisho wa Hukmu Juu ya Mfungwa Wa Kiislam)*

Na Ingawa Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii ametofautisha baina ya Sala ya Khofu baina ya Mtu anaefukuzwa na Maadui zake na Mtu anaewafukuzia Maadui zake, lakini kwa upande wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Khofu inayohisabika katika hili ni kuhusiana na Kuikosa Sala, na hivyo hua haiangaliwi kama Mtu ni mwenye Kukimbia au ni mwenye Kukimbiza.'**Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Ibn Habib Al Maliki.

Lakini kwa upande wa Imam Abu Is-haq Al Fazari basi yeye amesema kua: '**Imam al Awzai amesema kua Kama Watu wanaowakimbilia Maadui zao watakhofia kua Kama watashuka kutoka Juu ya Vipando vyao na kuamua Kusali Ardhini basi Watawakosa Maadui zao, basi hua Wanaruhusika Kusali Juu ya Vipando vyao na kuelekea Upande wowote ule walioelekea. Na hiini kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: Ushindi hautokoseshwa kwa Waislam pale watakapokua Wanawafukuzia Maadui zao.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Jarir At Tabari Al Shafii na Imam Ibn Abd Al Barr Al Maliki basi wamenukuuHadith ya Imam Al Awzai aliesema kua: '**Sharhabil Ibn Samit aliwaambia Watu wake kua: Msisali Al Fajir isipokua Juu ya Farasi wenu**. **Hivyo Al Ashtar An Nakhai akashuka chini kutoka juu ya Farasi wake na kisha akasali Juu ya Ardhi**. **Hivyo Sharhabil akasema kua An Nakhai ni Mvunjaji umoja wa Waislam ambae ni mwenye kumuasi *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***

Na Imam Ibn Abi Shaybah amenukuu pia Kisa hiki na kusema: '**Thabit Ibn Samit alikua na Khofu na hivyo Akasali huku akiwa Juu ya Farasi wake, hivyo An Nakhai hakua na khofu na akasali chini Ardhini, na Hivyo An Nakhai amekua ni mwenye Kuasi maamrisho ya Kiongozi wake.'**

Na Imam Al Battal anasema kua: '**Kama ingekua umepatikana Ushahidi wa Hadith kuhusiana na wale waliosali juu ya Vipando basi ingekua kuna Uthibitisho wenye nguvu juu ya jambo hilo, na kama haikupatikana basi kilichofanyika hapa ni hali ya Uthibitisho wa Makisio tu kama vile ambavyo inapokua Inaruhusika Kuchelewasha Sala kutoka katika Mda wake uliowekewa, basi**

ndivyo pia imeruhusika kwa Mtu mwenye Khofu kuacha baadhi ya Nguzo za Sala na Kusali kuashiria.

Na akasema Imam Ibn Munir Al Iskandary kuhusiana na hili kua: '**Kile kilichowazi katika uthibitisho ni kutokana na Mtizamo wa kua amrisho la Kuharakisha ni lenye kupelekea Alieamrishwa kuikosa Sala yake, kama ilivyotokea kwa Baadhi ya Masahaba, ambapo Badala yake hua ni Kusali juu ya Kipando kama ilivyotokea kwa Masahaba, na hii ni kwa sababu Kushuka kutoka katika Kipando hua kunaondoa Malengo ya Kuwahi Kufika anakokimbilia Mhusika.**

Na hivyo katika hali kama hii basi kushuka kutoka kwenye Kipando hua ni Kosa kwa sababu hua ni kupingana na Umaalum wa Amrisho la Kuharakisha, kwani Kuchelewa kwao kutatokana na Kupingana na amrisho.

Hivyo Masahaba wakawa wanachanganya uthibitisho wa amrisho la Kuharakisha na Amrisho la Kusali katika wakati wa Sala, na hivyo ndio wakaamua Kusali juu ya Kipando.

Na hivyo ni kama tukihesabu kua Walishuka kutoka kwenyw vipando basi hii itakua ni kinyume na walivyoamrishwa kuharakisha, na Masahaba walikua si wenye sifa ya Kumpinga *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Kwa sababu Masahaba waliocheleweshe Sala hadi walipofika Banu Quraydha.Hawakukoselewa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusali nje ya mda na wala wale waliosali Juu ya vipando vyao kwa kuashiria hawakukoselewa pia, hivyo Kuisali Sala Juu ya Kipando katika wakati wa Khofu hua ni bora kuliko Kuisali nje ya wakati wake, wa Allahu Aalam. *(Fat-h Al Barr, Al Wajiz Fi Ahkam Al Asir Al Muslim)*

Ama kuhusiana na Hadith inayozungumziwa hapa ya Banu Quraydha katika Kukisia kuhusiana na Kuruhusika Kusali juu ya Kipando kwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* waliokua kwenye amrisho la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* la Kukimbilia kwa Banu Quraydha ni ile Hadith maarufu isemayo:

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ مُحَمَّدِ بْنِ أَسْمَاءَ، حَدَّثَنَا جُوَيْرِيَةُ بْنُ أَسْمَاءَ، عَنْ نَافِعٍ، عَنِ ابْنِ عُمَرَ ـ رضى الله عنهما ـ قَالَ قَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم يَوْمَ الأَحْزَابِ " لاَ يُصَلِّيَنَّ أَحَدٌ الْعَصْرَ إِلاَّ فِي بَنِي قُرَيْظَةَ ". فَأَدْرَكَ بَعْضُهُمُ الْعَصْرَ فِي الطَّرِيقِ، فَقَالَ بَعْضُهُمْ لاَ نُصَلِّي حَتَّى نَأْتِيَهَا. وَقَالَ بَعْضُهُمْ بَلْ نُصَلِّي، لَمْ يُرِدْ مِنَّا ذَلِكَ، فَذُكِرَ ذَلِكَ لِلنَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَلَمْ يُعَنِّفْ وَاحِدًا مِنْهُمْ.

Amesema AbdAllah Ibn Muhammad Ibn Asmaa kua amesema Juwwayriyyat Ibn Asmaa kua Amesema Nafii kua amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua, katika Vita vya Ahzab (Vya Khandak) basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwatuma Masahaba zake na kuwaambia kua: 'Asisali hata Mmoja wenu miongoni mwenu Sala ya Al Asr Isipokua baada ya Kufika Banu Quraydha.'

Hivyo Sala ya Al Asr ikawakuta Masahaba wakiwa Njiani, na Miongoni mwao wakasema: 'Sisi Hatutosali Hadi tutakapofika Banu Quraydha.'

Na wengine wakasema 'Sisi Tutasali hapahapa ilipotukuta (Juu ya Farasi wetu) kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumaanisha hivyo.'

Na habari hii ilipomfikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi hakuwakosoa wowote miongoni mwao'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Hivyo basi katika Hadith hii Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua chini ya amrisho la Kukimbilia Banu Quraydha, huku ndani yake ikiwa mna amrisho la Sala.Na hivyo Masahaba wakaona kua kama Wakisimama na Kusali basi itakua Wameasi amrisho la kuharakisha, na ndio maana tukaambiwa kua tukasali Banu Quraydha kutokana na umuhimu wa Kutakiwa kuwahi hivyo tutasali kwa Banu Quraydha.

Ambapo hapo hapo wengine wakaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha hivyo kutokana na kua tusisimame sehemu yeyote kwani tutachelewa, hivyo wakaamua kua Wasali juu ya Farasi wao huku wakiwa safarini bila kusimama sehemu yeyote.

Na amesema Muwaffaq Ad Din Imam Abu Muhammad Ahmad Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Kama ikiwa Mtu atakua ni mwenye Kukimbia kutokana na Maadui zake, Kutokana na akulichoruhusika Kukikimbia Kukimbia Mafuriko, Mnyama Mkali anaetaka Kumdhuru, Mripuko wa Moto ambao ni Mkubwa sana usiopekika basi Mtu huyo hua ni mwenye kuruhusika Kusali Sala ya Khofu kubwa, iwe Khofu hio ni kwa ajili ya Nafsi yake, Familia yake au Mali yake.**

Na Kama ni Mfungwa anaeikhofia Nafsi yake, Mtu aliejificha kwa ajili ya Kuihifadhi na kuiokoa Nafsi yake, basi anaruhusika kusali Sala ya Khofu kwa namna atakavyoweza Ambapo huo ni Mtizamo wa Muhammad Ibn Hasan.

Na amesema Iman Al Shafii kua Mtu mwenye hali kama hizo hua anatakiwa Kusali kwa kadri atakavyoweza lakini akipata Nafasi ya Kua Salama basi itambidi airudie Sala hio. **Na hii hua si sahih kwa sababu mwenye Khofu huruhusika Kusali kwa kadri awezavyo hivyo hua hatakiwi kuirudia Sala hio tofauti na Mtu anaekimbia kuiokoa Nafsi yake.**

Na pia Wanazuoni wanakubaliana kua hua hakuna Tofauti baina ya Sala ya Mwenye mwenye kuishi katika Mji husika anaestahiki Kusali Sala ya Kawaida na Mtu mgeni anaestahiki kusali Sala ya Safari kuhusiana na Jambo hili la Sala ya Khofu.

Na hii ni kwa Sababu Sala hii imeruhusika kutokana na Khofu ya Kukabiliana na Kifo Jambo ambalo hua ni lenye kua na Hali sawia kwa watu wote iwe Mgeni wa sehemu husika au mwenyeji.

Kwani wote huani wenye kuhitajia Kujiokoa na Mauaji kama vile mtu ambae anaekimbilia Mlimani kwa ajili ya Kukimbia Maji ya Mafuriko yasimkute. Basi na Mwenye Kumkimbia Adui hua ni mwenye kuweza kukimbilia kwenye sehemu yenye Ngome akajificha ili kujiokoa kutokana mashambulio Dhidi ya Maadui.

Hivyo Mtu hua anaruhusika Kusali Sala katika hali ya Khofu katika Hali hizi kwa sababu kufanya hivyo kumeruhusiwa kutokana na mazingira stahiki kama haya.'*(Al Mughni)*

Hivyo kutorudia Sala hio hua nikulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kutokana na hadith ya Ya'ala Ibn Murrah *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pamoja na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhu* walikua Safarini na wakafika kwenye sehemu ambayo ni Nyembamba, huku wao wakiwa juu ya Farasi wao na Ardhi**

ilikua Imejaa Matope mengi sana.Na wakati wa Sala ukaingia hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuamrisha Mmoja kati ya Masahaba zake kua Aadhini, na baada ya Adhana basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatangulia mbele pamoja na Farasi wake na akasalisha huku akiwa juu ya Farasi wake.Na aliinamisha Kichwa chake katika wakati wa Kurukuu na Kusujudu, huku akiwa ni mwenye kuinamisha zaid kichwa chake katika wakati wa kusujudu kuliko katika kurukuu.'

Lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Maliki na Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua Inabidi Mtu husika arudie Sala hio pale itakapokua yuko katika hali ya usalama, na hii ni kutokana na aya pale iliposema:

﴿فَإِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا أَوْ رُكْبَانًا ۖ فَإِذَا أَمِنتُمْ فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُون﴾

Fa-in khiftum farijalan aw rukbanan fa-idha amintum faodhkuroo Allaha kama AAallamakum ma lam takoonoo taAAlamoona*(Surat Al Baqara 2:239)*

*Tafsir: **Lakini Kama Mkiwa na Khofu Salini mkiwa mmesimama Kwa Miguu au kwa Juu ya Kipando Na Hivyo Pale Mtakapokua Salama Basi Mkumbukeni Allah Katika Sala Kama Mlivyofundishwa Ambavyo Mlikua hamjui Hapo Kabla.***

Na anasema Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Kama atakua anadaiwa na hakua na uwezo wa kulipa, na akawa anafukuzwa na Mtu anaemdai basi Mtu huyo anaedaiwa hua anaruhusika Kusali Sala ya Khofu.'***(Al Bayan Fii Madhhab Al Shafii)*

Na akasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Kama ikiwa Mtu amejificha kutokana na kuwakimbia Maadui zake, na anaogopa kua akisimama Watamuona basi anaruhusika Kusali Sala ya Khofu kwa kukaa Kitako, na kama anahisi kua katika kukaa kwake ataonekana basi anaruhusika Kusali kwa Kulala, na kama haiwezekani basi na asali kwa kadiri atakavyoweza**'*(Al Mughni)*

Kwani tunakumbushana kua Sala ya Khofu tunayoizingumzia hapa si ile Sala ya Khofu, bali ni Sala katika Wakati na mazingira ya khofu.

Kwa sababu Sala ya Khofu ni Sala tofauti ambayo tutaizumgumzia pia, ambayo hua Inasaliwa kwa Kufupisha Sala ya Kawaida mbele ya Maadui, katika Mapigano ya Wajibu na yaliyoruhusika Kisharia kama Jihad Fii Sabili Allah.

Ila hapa tunazungumzia Sala ambayo Mtu inabidi Asali huku akikimbia hatari au amejificha n.k. Kwa mfano amejificha Nyuma ya Jabali au Ukuta ambao sio Mrefu na hivyo akisimama basi atatunguliwa. Hivyo katika hali kama hii anaruhusika Kusali akiwa amekaa Kitako n.k.

Na hii ni kwa sababu Aya ya 239 ya Surat Al Baqara ilivyoamrisha hili ambayo tunaona kua ni yenye kumalizia kwa kusema:

﴿فَإِذَا أَمِنتُمْ فَاذْكُرُوا اللَّهَ كَمَا عَلَّمَكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُون﴾

Fa-idha amintum faodhkuroo Allaha kama AAallamakum ma lam takoonoo taAAlamoona*(Surat Al Baqara 2:239)*

Tafsir: ***Hivyo Pale Mtakapokua Salama Basi Mkumbukeni Allah Katika Sala Kama Mlivyofundishwa Ambavyo Mlikua hamjui Hapo Kabla.***

Ambayo ni yenye kuonesha Kuruhusika Kurukuu na Kusujudu kwa kuashiria tu katika wakati wa hali ya Khofu.

Ambapo amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Yanapoanza Mapigano basi Sala hua ni Kwa Dhikr na kwa ishara tu.**' (Imam At Tabari)

Na imetajwa katika Al Ibanah kua: '**Kama Mtu akiwa anakimbia kutokana na Kutakisa kulipiziwa Kisasi, basi Hua anaruhusika Kusali Sala ya Khofu, kwa Sababu ndani yake hua ni mwenye kutegemea Usamehevu.'***(Al Bayan Fi Madhhab Al Shafii)*

Hivyo basi kwa Kuhitimisha tunaona kua Sala ya Wakati wa Khofu hua inaruhusika pale inapokua:

1-Mtu anakhofia Uhai wake kutokana na Maadui, Madhara ya hatari ya Moto, Mafuriko, Gharika,Theluji, Wanyama wa Hatari kama Nyoka, Simba n.k.

Ambapo huu ni Mtizamo Unaokubalika zaidi kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Al Shafii na Imam Ahmad.

2-Mtu anaewafukuzia Maadui zake Wasitoweke au anaewakimbia Maadui zake wasimkamateAmbapo hapa kunabaadhi ya Wanazuoni Wanasema kua Mwenye kuwafukuzia Maadui Zake basi hua haja ya Kusali Sala ya Khofu miongoni mwao ni Imam Al Shafii na Imam Abu Hanifa. Kwani amesema Imam Al Shafii kua: Anaemfukuzia Adui yake basi Hatakiwi Kusali Sala ya Khofu.'*(Al Bayan Fi Madhhab Al Shafii)*

Na kwa wanaosema kua anaruhusika Kusali Sala ya khofu ni Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik na Ahmad Ibn Hanbal n.k

3-Mtu anaekimbilia Katika Arafah na hivyo kua ni mwenye Khofu ya kua huenda akaikosa Arafah basi anaruhusika Kusali Sala ya Khofu.

Ambapo Huu ni Mtizamo unaokubalika zaidi wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, akiwemo Shaykh Ibn Taymiyyah na mwanafunzi wake ambae ni Imam Ibn Al Qayyim Al Jawzy pia ndio Mtizamo wa baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii akiwemo Sultan Al Ulamaa Shaykh Ul Islami Imam Izza Ad Din Ibn Abd Salam Al Shafii.

YALIYORUHUSIKA NDANI YA SALA – JAM'AA- KUJUMUISHA SALA.

❖❖❖❖

Wamesema Imam Al Bukhari, Imam Muslim na Imam An Nasai kua:

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ عَبْدِ الْعَزِيزِ بْنِ أَبِي رِزْمَةَ، - وَاسْمُهُ غَزْوَانُ - قَالَ حَدَّثَنَا الْفَضْلُ بْنُ مُوسَى، عَنِ الأَعْمَشِ، عَنْ حَبِيبِ بْنِ أَبِي ثَابِتٍ، عَنْ سَعِيدِ بْنِ جُبَيْرٍ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه

وسلم كَانَ يُصَلِّي بِالْمَدِينَةِ يَجْمَعُ بَيْنَ الصَّلاَتَيْنِ بَيْنَ الظُّهْرِ وَالْعَصْرِ وَالْمَغْرِبِ وَالْعِشَاءِ مِنْ غَيْرِ خَوْفٍ وَلاَ مَطَرٍ . قِيلَ لَهُ لِمَ قَالَ لِئَلاَّ يَكُونَ عَلَى أُمَّتِهِ حَرَجٌ .

Amesema Muhamamd Ibn Abd Abu Rizmat kua amesema Gazwan kua amesema Al Fadhl Ibn Musa kua amesema Habib Ibn Abi Thabit kua Said Ibn Jubayr kua amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alichanganya Sala alipokua Safarini katika Mji wa Madina. Hivyo alichanganya Sala ya Dhuhr na Asr, na Sala ya Maghrib na Isha, katika Wakati ambao ilikua hakuna Khofu wala Mvua Hivyo Abd Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anh*u akailizwa kwa kusema: Jee ni Kitu gani kilichompelekea kufanya hivyo?.'**

Abd Alla Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Hakutaka Kuuhangaisha Ummah wake.'*(Sunnan An Nasai)*

Na pia amesema Imam An Nasai kua:

أَخْبَرَنَا مُحَمَّدُ بْنُ سَلَمَةَ، وَالْحَارِثُ بْنُ مِسْكِينٍ، قِرَاءَةً عَلَيْهِ وَأَنَا أَسْمَعُ، - وَاللَّفْظُ لَهُ - عَنِ ابْنِ الْقَاسِمِ، قَالَ حَدَّثَنِي مَالِكٌ، عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ الْمَكِّيِّ، عَنْ أَبِي الطُّفَيْلِ، عَامِرِ بْنِ وَاثِلَةَ أَنَّ مُعَاذَ بْنَ جَبَلٍ، أَخْبَرَهُ أَنَّهُمْ، خَرَجُوا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَامَ تَبُوكَ فَكَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَجْمَعُ بَيْنَ الظُّهْرِ وَالْعَصْرِ وَالْمَغْرِبِ وَالْعِشَاءِ فَأَخَّرَ الصَّلاَةَ يَوْمًا ثُمَّ خَرَجَ فَصَلَّى الظُّهْرَ وَالْعَصْرَ جَمِيعًا ثُمَّ دَخَلَ ثُمَّ خَرَجَ فَصَلَّى الْمَغْرِبَ وَالْعِشَاءَ

Amesema Muhammad Ibn Salamah, kua amesema Kharith Ibn Miskina kua alisomewa na mimi nimesikia Ibn Qasim kua amesema Malik kua amesema Abi Zubayr Al Makki kua amesema Abu Tufayl Amr Ibn Wathilah kua amesema Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* kua:'Tulitoka na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Mwaka wa vita vya Tabuk. Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akichanganya Sala ya Adh Dhuhr na Al Asr na Maghrib na Isha, Na alikua akicheleweshe Sala Siku moja na kisha hutoka na Kusali Dhuhr na Al Asr pamoja na kisha hurudi ndani na kutoka tena na kusali Maghrib na Isha.'*(Sunan An Nasai)***

Na amesema Imam Al Bukhari kua:

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، قَالَ حَدَّثَنَا سُفْيَانُ، عَنْ عَمْرٍو، قَالَ سَمِعْتُ أَبَا الشَّعْثَاءِ، جَابِرًا قَالَ سَمِعْتُ ابْنَ عَبَّاسٍ ـ رضى الله عنه ـ قَالَ صَلَّيْتُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم ثَمَانِيًا جَمِيعًا وَسَبْعًا جَمِيعًا. قُلْتُ يَا أَبَا الشَّعْثَاءِ أَظُنُّهُ أَخَّرَ الظُّهْرَ وَعَجَّلَ الْعَصْرَ وَعَجَّلَ الْعِشَاءَ وَأَخَّرَ الْمَغْرِبَ. قَالَ وَأَنَا أَظُنُّهُ

Na amesema Ali Ibn Abd Allah Kua amesema Sufyan kua amesema Amr kua amesema Abu Shatha Jabir Ibn Zayd kua amesema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

Nilisali mimi na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Rakaa nane za Dhuhr na Al Asr na kisha nikasali Rakaa Saba Za Maghrib na Isha pamoja.

Hivyo Amr akamuuliza Imam Jabir Ibn Zayd kwa kusema: 'Ewe Abu Shaatha Nafikiri mimi kua labda Alisali Sala Ya Adhuhuri kwa kuicheleweshа na Sala ya Al Asr kwa kuiwahisha. Na akasali Sala ya Maghrib kwa kuicheleweshа na Isha kwa Kuiwahisha.Ambapo Imam Jabir Ibn Zayd akasema: Hata mimi nafikiria hivyo hivyo*(Sahih Al Bukhari)*

Na katika Sahih Muslim hadith hii ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kupitia kwa Imam Jabir Ibn Zayd imenukuliwa na Imam Ayoub Al Sakhtiyani ambae alimuuliza Imam Jabir Ibn Zayd kawa kusema: Inawezekana ikawa Kujumuisha huko kwa Sala ilikua ni kwa Sababu ya Mvua kubwa?Ambapo Imam Jabir Ibn Zayd akasema: 'Naam inawezekana ni kwa sababu ya kunyesha Mvua Kubwa.''*(Sahih Muslim)***

Naam..hizi ni baadhi ya Hadith tulizoanza nazo ambazo zenye kutuonesha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alijumuisha Sala, kwa sababu ya kuwepo kwa Dharura maalum. Kwani ilikua si kawaida yake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kucheleweshа Sala isipokua pale inapokua kuna Dharurah na hii ni kwa sababu ya kuwarahisishia Dini Waislam ili kuweza kufanya Ibada kwa wepesi kwa kadri watakavyoweza.

Na amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:

كانَ رَسولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ إذَا ارْتَحَلَ قَبْلَ أنْ تَزِيغَ الشَّمْسُ، أخَّرَ الظُّهْرَ إلى وقْتِ العَصْرِ، ثُمَّ نَزَلَ فَجَمع بيْنَهُمَا، فإنْ زَاغَتِ الشَّمْسُ قَبْلَ أنْ يَرْتَحِلَ صَلَّى الظُّهْرَ ثُمَّ رَكِبَ

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anapotaka Kusafiri kabla ya Jua Kua Utosini basi aliicheleweshа Salat Adh Dhuhr hadi wakati wa Al Asr**. **Ambapo hushuka kutoka Juu ya Kupando chake na kisha Husali kwa kuzijumuisha pamoja.**

Na kama ikiwa ameanza Safari wakati Jua Limeshapita Utosini kabla ya Safari basi husali Salat Adh Dhuhr na Al Asr kwa kuzijumuisha pamoja kisha ndio huanza Safari yake.'*(Sahih Bukhari)*

Ambapo hii pia ni hadith inayoelezea kuhusiana na aina mbili tofauti zinazoruhusika Kuchanganya Sala mbili katika wakati wa kipindi cha Salam moja. Na aina ya kwanza hua ni *Taqdiim* yaani kujumuisha Sala za vipindi viwili kwa pamoja ndani ya kipindi cha maanzo cha Sala baina ya Sala mbili husika yaani Kusali Sala ya Adh Dhuhr na Al Asr katika wakati wa Sala ya Adh Dhuhr, na kusali Sala ya Maghribi na Isha katika wakati wa Sala ya Maghrib.

Na aina ya pili hua ni Taakhir yaani kucheleweshа Sala Kwa kuzisali Sala mbili ndani ya kipindi Kimoja cha Sala ya pili baina ya Sala mbili. Yaani Kusali Sala ya Adh Dhuhr katika wakati wa Sala ya Al Asr na pia kusali Sala ya Maghrib na Al Isha katika Kipindi cha Sala ya Al Isha.

Ambapo ndani yake Sala hizi hua ni zenye kufupishwa, yaani kwa Kila Sala ya Rakaa nne basi husaliwa Rakaa mbili tu badala yake, isipokua Salat Al Maghrib ambayo ni yenye Rakaa tatu. Na hivyo hua haifupishwi, kama ilivyokua kwa Sala ya Al Fajir ambayo nayo pia hua haifupishwi kwa sababu ina Rakaa mbili na pia Salat Al Fajr hua haijumuishwi bali hua inasaliwa peke yake kama kawaida. Na vile vile pia hua hairuhusiki kuchanganya Salat Al Asr na Salat Al Maghrib. Na katika kuchanganya Sala

hizi hua haitakiwi iwe umepita mda mrefu baina yao, kwani ukipita basi itabidi mtu asali sala husika kiukamilifu.

Kwani amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Inaruhusika Kuchanganya Sala, kama Ad Dhur na Al Asr kwa Kuziwahisha au kwa kuzichelewesha, na pia kwa Salat Al Maghrib na Salat Al Isha pale inapokua Mtu yuko katika Safari ndefu.Na inaruhusika pia kuzijumuisha Sala kutokana na Mvua kubwa, Theluji na pia Kimbunga cha Upepo kama wa Barafu n.k.'***(Minhaj Talibin)*

Na ingwa huo ndio mtizamo unaotegemewa zaidi ndani ya Madhhab ya Imam Al Shafii. '**Lakini pia kuna baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wenye Mtizamo usemao kua: Inaruhusika Kuchanganya Sala kutokana na Maradhi, akiwemo Ash-Sheykh, al-Imam, al-'Alim, al-'Allamah, as-Salih, az-Zahid, ar-Rabbani Shihab ad-Din Ahmad Ibn Hussein Ibn Ali Ibn Raslan ar-Ramli '***(Safwa Zubbad)*

Na pia kuna mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii aliouelezea Imam An Nawawi usemao kua: '**Amesema Imam Al Khattabi Al Shafii kua amesema Imam Al Qaffal Al Kabir Al Shashi Al Marwazi Al Shafii kua, amesema Imam Abu Is-haq Al Marwazi Al Shafii kua: Inaruhusika kuchanganya Sala kwa Mtu ambae ni mwenyeji wa Mji bila ya kutokana na kuwepo kwa hali ya Mvua au Maradhi, ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Ibn Al Mundhir.'** *(Rawdhat Talibin)*

Na pia kuna Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii aliouelezea Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani usemao kua: '**Kuna baadhi ya Wanazuoni wametoa Fatwa isemayo kua Kuchanganya Sala kwa Mtu asiekua Safarini bila ya kua na dharura hua kunaruhusika.Na miongoni mwa waliosema hivyo ni Imam Muhammad Ibn Sirin, Imam Rabiah, Imam Al Ashabi, Imam Ibn Al Mundhir Al Nishapuri na Imam Al Qaffal Al Kabir, na Imam Al Khattabi amenukuu haya kutoka kwa Kutoka kwa baadhi ya Wanazuoni.'** *(Fat-h Al Barr)*

Na akasema tena Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi al Shafii kua: **'Kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu ya Al Shafii, Madhhab ya Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Malik, Madhhab ya Imam Ahmad na wengi miongoni mwa Wanazuoni basi ni kua Hairuhusiki Kuchanganya Sala bila ya kua Safarini au kua katika hali ya Khofu au katika Maradhi.**

Lakini hata hivyo Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri amenukuu kutoka kwa baadhi ya Wanazuoni ambao wamesema kua Inaruhusika Kuchanganya Sala bila ya hata kua na Sababu Maalum.

Na Imam Ibn Al Mundhiri amesema kua amesema Imam Ibn Sirin kua Inaruhusika kufanya Hivyo kutokana na hitajio ila isiwe kua Mtu kufanya kua ndio mazoea yake ya kawaida.'*(Al Majmuu)*

Na anasema Imam Ibn Habib Al Maliki kua: **'Inaruhusika kuchangnya Sala bila ya hata kua na sababu maalum.'**

Na Imam Ibn Arafah Al Maliki amesema kua: **'Mmoja kati ya Wanazuoni wetu alikua ni mwenye kuchanganya Sala pale anapokua anataka kuenda kwenye Hammam.'**

Imam Ibn Qudamah amesema tena kua: **‘Ama kuhusiana na hali ya hewa ya Upepo Mkali, Baridi kali au Kiza kikubwa cha Usiku wa Baridi basi kuna mitizamo miwili juu yake, ambapo wa kwanza ni kama alivyosema Imam Al Amidi kua inakubalika na huu ndio mtizamo Sahih zaidi kama alivyoelezea Umar Ibn Abd Al Azizi kwa sababu Upopo Mkali, Baridi Kali, Kiza Kizito, hua ni miongoni mwa Sababu za kuruhusika kutoenda Msikitini na kuchanganya Sala.’**

Na pia kuna mtizamo usemao kua hairuhusiki na hii ni kwa sababu Matope na Upepo hu ni vitu vyepesi ukilinganisha na Mvua kubwa. **Hivyo Kuchanganya Sala hua hakuruhusiki kwa jambo jengine lolote isipokua tuliyoyataja, ila Imam Ibn Shabramah amesema kua Kama ikiwakuna haja ya kufanya hivyo basi hua inaruhusika isipokua isiwe ndio Mazoea.’***(Al Mughni)*

Na Al Aalama Ibn Qasim Al Hanbal amesema kua: ‘**Inaruhusika kuchanganya Sala pale inapokua kuna matatizo au Ugumu.’** *(Hashiyah Al Rawdh Al Murabba)*

Na Imam Al Mardawi Al Hanbali akasema kua: ‘**Amesema Ahmad katika nukuu ya Muhammad Ibn Mashish kua: Kuchanganya Sala kwa Mwenyeji wa Mji, kama ikiwa ni kutokana na Hitajio la Dharura kama Maradhi au Jukumu la kazi.**’

Imam Al Mardawi anaendelea kusema kua : ‘**Na Al Qadhi amesema kuhusiana na majukumu ya kikazi yanamaanisha kuruhusika kuachana na Sala ya Jamaa kwa mfano kama itakua labda kama Mtu anajikhofia Nafsi yake au anakhofia kua atapoteza Mali yake.**

Ambapo kwa upande wa Shaykh Taqi Ad Din amechagua kuruhusika kuchanganya Sala hata kwa Wapishi, Wenye Mabekari, n.k ambao watakua na khofu kua Mali zao na Mali za wenzao zitadhulumiwa na kupotea.’*(Al Insaaf-Dar Al Ihya AlTurath)*

Na akasema Imam Al Buhuti Al Hanbali katika kuelezea yanayoruhusika kuchanganya Sala kua: ‘**Ni kwa Mtu anaeruhusika Asisali Sala ya Ijumaa wala ya Jamaa kutokana na Dharura kwa mfano kua na Khofu juu ya Uhai wake, Heshima yake, Mali yake au Kusababisha Madhara kwa Jamii ya watu anaoishi nao karibu, n.k hivyo humbidi kuchanganya Sala.’*****(***Kashf Al Qinaa)*

Kwani anasema Imam Muslim Ibn Hajjaj kua:

عن عبد الله بن شقيق قال: خطبنا ابن عباس يوماً بعد العصر حتى غربت الشمس وبدت النجوم، وجعل الناس يقولون الصلاة الصلاة. قال: فجاءه رجل من بني تميم لا يفتر ولا ينثني الصلاة الصلاة، فقال ابن عباس: أتعلمني بالسنة لا أم لك؟ ثم قال: رأيت رسول الله صلى الله عليه وسلم جمع بين الظهر والعصر والمغرب والعشاء. قال عبد الله بن شقيق فحاك في صدري من ذلك شيء، فأتيت أبا هريرة فسألته، فصدق مقالته

Amesema Abd Allah Ibn Shaqiq kua: Siku moja Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* alitutolea Khutba baada ya Sala ya Al Adh Dhuhr hadi Jua likazama na Nyota zikaanza kuonekana: **Watu wakaanza kusema Salaa, Salaa!**

Na kisha Mmoja kati ya Watu wa Banu Tamim akamsogelea Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*Huku akiwa ni mwenye kusema bila kusita Salaa! Salaa!

Hivyo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akamgeukia Mtu huyo na kusema: Na ulaaniwe! yaani Unanifundisha Mimi Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akaendelea kusema: Hakika mimi nimemuona R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,*akijumuisha Sala ya Adh Dhuhr, Al Asr, Magrib na Al Ishaa.

Abd Allah Ibn Shaqiq anaendelea kusema kua: Hakika mimi sikupenda aliyoyasema Abd Allah Ibn Abbas*Radhi Allahu Anhu,* na hivyo nikamfuata Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu,* na kumuuliza kuhusiana na ukweli wa aliyoyasema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*

Na Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* akathibitisha kua aliyoyasema Abd Allah Ibn *Abbas Radhi Allahu Anhu* kua ni Ukwel*i(Sahih Muslim)***

Naam..bado tuko katika kuangalia kuhusiana na Kuruhusika Kujumuisha Sala ndani ya kipindi kimoja kulingana na Vithibitisho vya Hadith na Mitizamo ya Wanazuoni. Ambapo tunaona kua Ingawa Kuna Mitizamo tofauti juu yake lakini kuna kukubaliana kua Haifai Kuchanganya Sala kwa Mazoea ya kua ndio Kawaida. Ambapo anasema Imam Ibn Abi Shaybah kua:

عن أبي بن عبد الله قال: جاءنا كتاب عمر بن عبد العزيز (لا تجمعوا بين الصلاتين إلا من عذر)

Amesema Abu Ibn Abd Allah kua: Sisi tulipokea Barua kutoka kwa Umar Ibn Abd Al Aziz ambayo ilikua ikisema kua:Msichanganye Sala isipokua pale mtakapokua Mna Udhuru.*(Musanaf Ibn Abi Shaybah)*

Na kuhusiana na Mgonjwa basi anasema Imam Muhammad Ibn Bahadur Ibn Abd Allah Al Zarkashi Al Shafii anasema kua: '**Ama kuhusiana na Kuchanganya Sala basi kwa upande wa Imam Muhammad Idris Al Shafii ana Qawlayn - Kauli mbili juu yake - Kua Inaruhusika Kuchanganya Sala kutokana na Maradhi ambao ni Mtizamo wa Imam Al Shafii uliotajwa kwenye Mukhtasar Al Muzani.'**

Ambapo hivonivyo pia alivyosema Imam Al Adhrai, na tunapozungumzia kitabu cha Mukhtasar Al Muzani basi ni Kitabu cha Imam Al Muzani ambae ni Mwanafunzi wa Imam Al Shafii.Na hii ni kutokana na Hadith ya Hamnat Bint Jahsh *Radhi Allahu Anha* isemayo kua:

قال المؤلف رحمه الله: [حدثنا زهير بن حرب وغيره قالا: حدثنا عبد الملك بن عمرو حدثنا زهير بن محمد عن عبد الله بن محمد بن عقيل عن إبراهيم بن محمد بن طلحة عن عمه عمران بن طلحة عن أمه حمنة بنت جحش رضي الله عنها قالت: كنت أستحاض حيضة كثيرة شديدة، فأتيت رسول الله صلى الله عليه وسلم أستفتيه وأخبره، فوجدته في بيت أختي زينب بنت جحش رضي الله عنها فقلت:

(يا رسول الله! إني امرأة أستحاض حيضة كثيرة شديدة فما ترى فيها؟ قد منعتني الصلاة والصوم؟ فقال: أنعت لك الكرسف فإنه يذهب الدم، قالت: هو أكثر من ذلك.

قال: فاتخذي ثوباً، فقالت: هو أكثر من ذلك، إنما أثج ثجاً.

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: سآمرك بأمرين أيهما فعلت أجزأ عنك من الآخر، فإن قويت عليهما فأنت أعلم.

قال لها: إنما هذه ركضة من ركضات الشيطان فتحيضي ستة أيام أو سبعة أيام في علم الله تعالى، ثم اغتسلي، حتى إذا رأيت أنك قد طهرت واستنقأت فصلي ثلاثاً وعشرين ليلة أو أربعاً وعشرين ليلة وأيامها، وصومي، فإن ذلك يجزئك، وكذلك فافعلي في كل شهر كما تحيض النساء وكما يطهرن، ميقات حيضهن وطهرهن، فإن قويت على أن تؤخري الظهر وتعجلي العصر فتغتسلين وتجمعين بين الصلاتين الظهر والعصر، وتؤخرين المغرب وتعجلين العشاء ثم تغتسلين وتجمعين بين الصلاتين فافعلي، وتغتسلين مع الفجر فافعلي، وصومي إن قدرت على ذلك، قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: وهذا أعجب الأمرين إلي).

Mwandishi, Mwenyezi Mungu amrehemu, amesema: Zuhair Ibn Harb na wengine walituambia: Abdul Malik Ibn Amr alituambia: Zuhair Ibn Muhammad alituambia, kwa idhini ya Abdullah Ibn Muhammad Ibn Aqil, kutoka kwa Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Talha, kutoka kwa ami yake Imran Ibn Talha, kutoka kwa mama yake Hamna binti Jahsh *Radhi Allahu Anha,* ambaye alisema:

Mimi nilikua na matatizo ya kutokwa na Damu nyingi sana na kwa mda mrefu katika Siku zangu, hivyo nikaenda kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumuulizia juu yake, nikakuta nyumbani kwa Dada yangu Zaynab Bint Jahsh *Radhi Allahu Anha.*

Ambapo nae akasema kua hio ni kutokana mzunguko unaotokana na Shaytan, hivyo nitakuamrisha juu ya mambo mawili, ambapo utakalo fanya kati yao basi litakutoshleza , hivyo kua katika Siku zako Kwa mda wa Sita au Saba, kisha Jitoharishe, na ukisha maliza basi Sali kwa mda wa Siku 24 au 23 na Funga na Usali, na hio itakutosheleza.

Fanya hivyo kwa kila mwezi kama wafanyavyo Wanawake wengine, na kama utaweza basi Kawilisha Sala ya Adh Dhuhr na iwahishe Sala ya Al Asr hivyo Jitoharishe na utakapokua Tohara basi Sali Sala ya Adhuhuri na Al Asr pamoja.

Na kisha Icheleweshe Sala ya Magharibi na iwahishe Sala ya Isha, yaani Jitojarishe kisha Changanya Sala mbili kwa pamoja,na kisha Jitoharishe kabla Kusali Alfajir, Hamna Binti Jahsh *Radhi Allahu Anha* akasema hi ndio inapendezea zaidi kwangu mimi.'*(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhii, Imam Ibn Majah)*

Hivyo mfano wa hadith ya Hamna Bint Jahsh *Radhi Allahu Anhu* umeruhusuksa Mtu mwenye Matatizo ya Afya kuchanganya Sala, ambapo amesema Imam Ibn Al Qayyim kuhusiana na hadithi hii kua**: 'Imam Ahmad Ibn Hanbal, Abdullah Ibn Al Zubayr Al Humaidi na Imam Is-haq Ibn Rahwayh ni wenyekuitumia Hadith hii kama uthibitisho.**

Ambapo Mtizamo huu wa Imam Al Shafii uliomo kwenye Mukhtasar Al Muzani ndio pia Mtizamo wa Imam Al Khattabi Al Shafii, Imam Al Sulayman Al Kurdi Al Shafii, Imam Al Ruyani Al Shafii, Imam Al Mawardi Al Shafii na Imam Ad Darimi Al Shafii.'*(Kifayat Al Akhyar, Mawahib Al Madaniyah na Rawda Talibin)*

Na ingawa huo ni Mtizamo wa Tatu ndani ya Madhhab ya Imam Al Shafii ambapo wa pili ni ule usemao kua: Inaruhusika Kuchanganya Sala bila hata ya sababu maalum lakini isiwe ndio kawaida tena kila siku, ambao ni Mtizamo wa Imam Ibn Sirin, Imam Rabiah, Imam Al Ashab, Imam Ibn Al Mundhir Al Shafii, Imam Al Qaffal Al KabirAsh Shashi Al Shafii, Imam Ibn Shabramah n.k.'*(Fat-h Al Barr,Al Qawwanin Al Fiqhiyyah)*

Lakini tunarudia tena kusema kua Mtizamo unaokubalika na kutegemewa zaidi na Madhhab ya Imam Al Shafii juu ya hili ni Mtizamo wa kwanza usemao kua: '**Inaruhusika Kuchanganya Sala, kama Ad Dhur na Al Asr kwa Kuziwahisha au kwa kuzicheleweshа, na pia kwa Salat Al Maghrib na Salat Al Isha pale inapokua Mtu yuko katika Safari ndefu.Na inaruhusika pia kuzijumuisha Sala kutokana na Mvua kubwa, Theluji na pia Kimbunga cha Upepo kama wa Barafu n.k.'***(Minhaj Talibin)*.

Ambao ndio pia Kauli ya pili ya Imam Al Shafii kama alivyosema Imam Al Athrai na Imam Al Zarkashi kuhusiana na Qawlayn juu ya jambo hili.

Kwani anasema Shaykh ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari Al Shafii kua:**'Na Kadhakika inaruhusika kuchanganya Sala kutokana na Mvua, Theluji na Mvua ya Mawe.'**(*Asn Matalib)*

Na akasema Imam Al Khatib Al Shirbini kua:**'Kinachodhihirika zaid katika haya kama ilivyosemwa kwenye Rawdhah basi ni kua Ruhusa ya Kuchanganya Sala hua ni Makhsusi kwa mwenye Kusali Msikitini au sehemu nyengine zaid katika Sala za Jamaa ambazo ziko mbali na Nyumba yake anayoishi, na hivyo hii hua ni kwa ajili ya kua asidhurike kutokana na Mvua, jambo ambalo ni tofauti na Mtu ambae yuko Jirani chini ya Msikiti kwani kwa mtu kama huyu basi Hukmu hii hua haimhusu.'***(Mughni Al Muhtaj)*

Hapa inabidi tufahamishane kua: '**Kuchanganya Sala kwa Dharurah kumeruhusiwa kwa ajili ya kuondoa Ugumu kwa Muislam na ingawa kuruhusiwa kwake kumethibitishwa na Vithibitiaho vya Sunna za Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* lakini hata hivyo hii haimaanishi kua Mtu mwenye kufanya hivyo atapata Malipo Zaidi.'**

Na hii ni kwa sababu anasema Imam Abu Zakarriyah Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Mbali ya kua imeruhusiwa kuchanganya Sala lakini hata hivyo Wanazuoni wanakubaliana kua kutochanganya Sala hua ni bora zaid.**'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na vile vile amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi, na Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Na Imam Ibn Abd Al Barr na pia Al Hafidh Imam Abu Fadhl Zayn Ad Din Abd Rahim Ibn Al Husayn Al Iraqi Al Shafii kua: '**Kuna Makubaliano ya Ijmaa ya Wanazuoni kua Ni Haram Kuchanganya Sala ya Alfajir na Sala nyengine yeyote, na pia ni Haram kuchanganya Sala ya Al Asr Na Salat Al Maghrib.'**

Na Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na Hukmu za Kuchanganya Sala kwa Dharura kua:

Anaechanganya Sala hua anatakiwa aanze na Sala za Mwanzoni, yaani katika kuchanganya Adh Dhuhr na Al Asr basi kwanza unaanza kwa kuisali Salat Al Dhuhr kisha unamalizia Al Asr, na baina ya Maghrib na Al Isha basi unaanza na Maghrib nakumalizia na Al Isha.

Anaechanganya Sala hua anatakiwa Kuzisali Sambamba yaani zisipishane kwa mda baina yao,hivyo kama ikiwa haiwezekani kuzichanganya kwa sambamba basi hua haitakiwi kuchanganya.

Ambapo huu ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Hanbal.

Wanazuoni wanakubaliana pia kua:Sababu ya Kuchanganya Sala iwe ni yenye kupatikana katika mwanzoni mwa wakati wa Sala ya kwanza baina ya Sala mbili zitakazochanganywa.

Ambapo huu ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Hanbal.

Wakati kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, wao anasema kua hili si sharti la kuchanganya Sala kulingana na mtizamo wao. Na Mtizamo huu pia ni wenye kukubalika kwa miongoni mwa baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na pia Shaykh Ibn Uthaymin

Na pia kuna baadhi ua Wanazuoni wasemao kua Hairuhusiki kuchanganya Sala ya Al Jumaa na Salat Al Asr. Na huu ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na pia ni wa baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wanakubaliana kuhusiana na Sharti la kua kwa yule mwenye Dharurah ya kuchanganya Sala na akataka kuchanganya Sala katika mfumo wa Taa'khir yaani Kucheleweshа kwa kuzisali katika Wakati wa kipindi cha Sala ya Pili, basi awe na nia hio tangu katika wakati wa Kipindi cha Sala ya Mwanzo baina ya Sala mbili hizo.

Ingawa kwa upande wa Imam Abu Hanifa yeye basi amesema kua: 'Hairuhusiki kuchanganya Sala ya Adh Dhuhr na Al Asr isipokua katika Ibada ya Hija katika Maeneo ya Arafah, katika Siku ya Arafah tu.'

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: 'Hairuhusiki kuchanganya Salat Al Dhuhr na Salat Al Asr kwa sababu ya Mvua.'

Na kwa upande wa Imam Al Shafii basi yeye amesema kua: 'Inaruhusika kuchanganya Sala ya Adh Dhuhr na Al Asr kwa sababu ya Mvua na hivyo inaruhusika kuchanganya Salat Al Jumaa na Salat Al Asr pia.'

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi amesema kua huo pia ndio Mtizamo wa As-hab wa Madhhab ya Imam Al Shafi.

Naam..hizo ni baadhi ya Maangalizo ya Tahadhari kuhusiana na kuchanganya Sala ama kuhusiana na baadhi ya Mifano ya Dharurah zinazokubalika kuruhusika kuchanganya Sala, kulingana na mazingira ya Maisha yetu ya leo basi ni pamoja na:

Wanaoruhusika kuchanganya Sala hua ni Madaktari Bingwa pale inapohitajika, yaani kwa mfano Daktari husika anahitajika kukaa ndani ya Chumba vha Upasuaji kwa ajili ya Kumfanyia upasuaji Mgonjwa au kuokoa Maisha ya Mgonjwa n.k

Upasuaji ambao utachukua Mda mrefu na hauwezi kukatishwa Basi hapa hua inaruhusika kwa Daktari husika kuchanganya Sala na hakuna ubaya wowote ndani yake kwa sababu ya Kuhifadhi Uhai wa Mtu na Malengo ya - Maqasid Al Shariyah - Makusudio ya Sharia Za Allah Subhanah wa Ta'ala ni hua ni Kuhifadhi Uhai, Kuhifadhi Ufaham, Kuhifadhi Imani ya Dini ya Kiislam, Kuhifadhi Mali na Kuhifadhi Kizazi.

Kwani Wanazuoni wanakubaliana kua Hua ni Sunnah kuchanganya Sala ya Adh Dhuhr na Al Asr katika wakati wa Adh Dhuhr katika Ibada ya Hijja kwenye Maeneo ya Arafah.

Na hua ni Sunnah kuchanganya Salat Al Maghrib na Salat Al Ishaa katika wakati wa Ibada ya Hija katika maeneo ya Muzdalifat. *(Imam Ibn Rushd, Imam Ibn Abd Al Bar)*

Na hua inaruhusika kuchanganya Sala katika wakati ambao Mtu anapokua Safarini, ndani ya masafa ya kilomoita 83 na Msafiri hua anaruhusika kuchagua apendavyo kama kucheleweshe au kuwahisha katika kuchanganya kwake huko.

Inaruhusika kuchanganya Sala kwa Mgonjwa.

Inaruhusika kuchanganya Sala kwa Mwanammke mwenye Istihadhah, yaani kutokwa na Damu katika kipindi ambacho si cha hedhi.

Inaruhusika Kuchanganya Sala katika wakati wa Mvua kali, Mafuriko, Kuanguka kwa Theluji, Aradhi Kujaa Barafu, Baridi Kali na Kuzagaa kwa Matope.

Inaruhusika Kuchanganya Sala kutoka na Khofu.

Inaruhusika kuchanganya Sala kwa Mwanamke mwenye Kunyonyesha mtoto ambae kila wakati anataka kunyonya n.k.

Inaruhusika kuchanganya Sala kwa kutokana na ugumu wa hali ya mazingira ya Ufanyaji Ibada ya Sala kulingana na maeneo husika.

Inaruhusika Kuchanganya Sala kwa Watu waliokua Safarini labda tusema kwa mfano wameganda kwenye Foleni kwa mda mrefu sana.

Inaruhusika kuchanganya Sala kwa Mtu kama mwanafunzi tuseme ambae ana mtihani ambao utachukua mda mrefu sana katika Kutahiniwa kwake.

Inaruhusika kuchanganya Sala kwa Mfungwa, Mtu alieko Mahbusi au Watu waliokua chini ya amrisho la kutotoka nje kutoka kwa Wenye Mamlaka.

Inaruhusika kuchanganya Sala kwa Mtu mwenye kusimamia Usalama wa Eneo au wa watu katika jamii.n.k. Ambapo yote haya hua ni kwa sharti la kua isiwe ndio mazoea.

Na kulingana na Mitizamo ya Madhhab ambapo tunaona kua: '**Kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua hairuhusiki pale Inapokua Mvua sio Kubwa, na Tope sio Nyingi'***(Mukhtasar Al Khalil)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua: **'Inaruhusika Kuchanganya Sala kutokana na Mvua itakapokua kubwa au ndogo ambayo itarowesha nguo na itakayoanza katika kipindi cha Sala ya kwanza, hivyo kama ikianza katika kipindi cha Sala ya pili basi hua haifai kuchanganya'***(Al Hawi Al Kabir Imam Al Mawardi na katika Al Majmuu pia)*

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao ni kua: '**Inaruhusika kuchanganya Sala kutokana na Mvua itakayorowesha nguo na kumzuia Mtu kuyoweza kutoka ndani mwake. Lakini kwa Mvua Nyepesi za Manyunyu na Rasharasha basi hua haiuhusiki kuchanganya Sala.**'*(Al Mughni Imam Ibn Qudamah, Al Iqna Imam Al Hajjawi)*

Na Mafaqih Saba wa Tabiina ambao ni Imam mwenye asili ya Kiafrika Imam Sayid Ibn Musayyeb, Imam Urwa Ibn Al Zubayr, Imam Qasim Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr Radhk Allahu Anhu, Imam Kharija Ibn Zaimyd Ibn Thabit Radhi Allahu Anhu, Imam Ubayd Allah Ibn Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Imam Sulayman Ibn Yasir na Imam Abu Bakr Ibn Abd Rahman: **'Wamesema kua : Inaruhusika kuchanganya Sala ya Maghribi na Isha tu kutokana na Mvua.'***(Dhakira Imam Al Qarafi)*

Kwani amesema Imam Ibn Qudama Al Maqdisi kua: '**Amesema Imam Al Adhram kua: Amir Ul Muuminin *Radhi Allahu Anhum*wote walikua wakichanganya Sala za Al Maghrib na Ishaa inaponyesha Mvua, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akichanganya pia. Na amesema Hisham Ibn Urwa kua: Mimi nilimuona Abaan Ibn Uthman akichanganya Sala mbili za Mahrib na Isha katika wakati wa Mvua. Na Urwa Ibn Az Zubayr na Abu Salamah Ibn Abd Rahman na Abu Bakr Ibn Abd Rahman pia walikua Wakichanganya Sala katika wakati wa Mvua, na wala msibishe kwa sababu hakuna mtu yeyote ambae alikua amewapinga katika Zama zao, kwa hivyo hua inakubalika**.'*(Al Mughni)*

Na amesema Imam Abd Razzaq Al Sanaani kua: **'Amesema Imam An Nafii kua Kila Khalifa alikua akichanganya Sala ya Maghrib na Ishaa katika wakati wa Mvua na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akichanganya pamoja nao katika siku za Mvua'***(Musannaf Ibn Abd Razzaq, na katika Sunnan Al Kubra ya Imam Al Bayhaqi pia)*

Na anasema Imam Al Baji kua: '**Hii ni maana ambayo mara nyingi huambatana na ugumu wa maisha. Ilikuwa na athari katika kuswali katika nyakati za faradhi, kama vile safari na maradhi.'***(Al-Muntaqa)*

Kutoka kwa Sahl Ibn Hanif amesema: **'Nilimsikia Abu Umamah akisema: 'Tulisali Salah ya Adhuhuri pamoja na Umar Ibn Abdul Aziz, kisha tukatoka mpaka tukaingia kwa Anas Ibn Malik*Radhi Allahu Anhu* na tukamkuta anasali Salah ya Al Asri, basi Akasema: 'Ewe ami, ni sala gani hii uliyo isali?':**

Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: 'Hii ni Sala ya Alasiri, na hii ni Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tuliyokuwa tukisali pamoja naye.''

Na Imaam Ahmad, Al Al Qadhi Al Husein na Imam Al-Mutawali wa Madhhab ya Imam Al Shafii wamehukumu kwamba inajuzu kuunganisha Salah kwa kuzileta mbele au kuzichelewesha kwa sababu ya maradhi, na hii ni kwa sababu ugumu wa kufanya hivyo ni mkubwa kuliko mvua.

Na kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kua: **'Kama ikiwa mvua itanyesha a kuendelea katika wakati wa kuchnagnya Sala mbili husika kwa mfano kata Sala ya Adh Dhuhur na kisha ikasimama, basi Salazote bili hua ni sahih na haitokua na haja ya kirudia Sala ya Al Asr.'**

Kwani amesema Imam Muhamamd Idris Al Shafii kua: 'Kama Mtu atasali moja kati ya Sala hizo wakati mvua inanyesha, na kisha akaanza kusali Sala nyengine yake wakati Mvua inaendelea Kunyesha, lakini Mvua hio ikakata kabla kumaliza Sala yake hio, basi Mtu huyo hua anatakiwa kuendelea na Sala yake hio, kwa sababu ya kutokana na kua kama vile ambavyo alikua na haki ya kuingia ndani ya Sala hio basi hua pia anayo haki ya kuimalizia Sala hio.'

Ama kwa upande mwengine basi amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿أَقِمِ الصَّلاَةَ لِدُلُوكِ الشَّمْسِ إِلَى غَسَقِ اللَّيْلِ وَقُرْآنَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْآنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا﴾

Aqimi al<u>ss</u>al<u>a</u>ta lidulooki alshshamsi il<u>a</u> ghasaqi allayli waqur-<u>a</u>na alfajri inna qur-<u>a</u>na alfajri k<u>a</u>na mashhood<u>a</u>n*(Surat Al-Isra 17:78)*

*Tafsir:**Simamisha Sala Kuanzia Mchana Linapopindukia JuaHadi Kinapoingia Kiza cha Usiku Na Someni Qur'an Katika Al Fajir Kwani kwa Hakika Kisomo cha Qur'an ya Al Fajiri hua Kinashuhudiwa.***

Naam..hii ni aya ambayo inamaamrisha Ibada ya Sala, na Ndani yake imetaja Nyakati tatu tofauti. Kwani kwanza Imeainisha wakati kwa kutumia neno Duluk. Ambapo neno Duluk linatokana na neno Dalaka lenye kumaanisha Kupindukia, Kutua, Kushuka kutoka juu na kuelekea kwa kuelemea upande wa Chini.

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Ad Din, Imam Al Mushaqqiqin, Sultan Al Mutakallimin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhar Ad Din Al Razi Al Shafii anasema kuhusiana na nalo neno hili kua: **'Wanazuoni wametufautiana kuhusiana na matumizi ya neno hili katika aya hii, kwani kuna wanaosema kua linamaanisha wakati ambao pale Jua linapoanza kugeukia Upande wa pili baada ya kua juu katikati**. **Na kuna wanaosema kua linamaanisha wakati ambao Jua linapozama.'**Na huo pia ndio Mtizamo wa Imam Al Qurtubi Al Andalus Al Maliki.

Na kwa upande wa Imam Ibn Attiyah basi yeye amesema kua: '**Neno Duluk linamaanisha kupindukia hivyohapa hua linaweza kutumika kwa maana ya Kupindukia katika wakati wa Adh Dhuhuri na pia ktika wakati wa Magharibi, hivyo ndani yake linajumuisha Sala nneambazo ni Adh Dhuhr, Al Asr, Maghrib na Al Ishaa.**

Ama kwa upande wa Sahaba Mwanazuoni Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema kua: '**Duluk hua linamaanisha Kuzama au kutua kwa Jua.'**

Ambapo Imam Ibn Jarir At Tabari basi yeye anasema kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **alikua akilitumia neno Duluk kumaanisha Kupindukia kwa Jua kutoka Juu na hivyo hii inamaanisha kua ni Adh Dhuhr.'**

Na kisha aya yetu hii ikaainisha Wakati mwengine kwa kutumia neno Ghusuq ambapo neno Ghusuq linatokana na neno Ghasaqa ambalo humaanisha Kuingia Kiza, Kutokua na uwezo wa kuonekana, Kutoonekana kitu na pia humaanisha Ubaridi usiokua na hata dalili ya joto yaani Ubaridi mkali sana wa kifo.

Na Wanazuoni ni wenye kukubaliana kua maana ya '**Neno Ghasaq iliyotumika hapa inamaanisha kua ni Kipindi cha Kuzama kwa Jua na kuchomoza kwa Nyota Mbinguni, yaani wakati** wa **Usiku.'***(Imam Ibn Jarir At Tabari)*

Hivyo Imam Fakhr Ad Din Al Razi anasema kua **'Kwa maana hio basi tukichukua mana ya kusimamisha Sala katika wakati wa Duluk kama kupindukia kwa Jua na Ghusuq kua ni kuchomoza kwa Nyota basi hapa kilichomaanishwa hua ni Sala nne yaani Adh Dhuhr, Al Asr, Maghrib na Al Ishaa.'**

Na kisha aya ikaainisha maneno Qur'ana Al Fajr yaani Kisomo cha Qur'an katika wakati wa Al Fajir. Ambapo maneno haya hua pia yanamaanisha kisomo cha Qur'an ndani ya Ibada ya Sala ya Al Fajir.

Kwani anasema Jarrah Allah, Imam Al Balagha Imam Abu Qasim Mahmud Ibn Umar Al Zamakhshari Al Hanafi kua: '**Qur'ana Al Fajr yaani Kisomo cha Qur'an cha Al Fajir kimenasbishwa na kuwekwa sambamba kimaana na Sala ya Al Fajir kutokana na kuainisha Umuhimu wa Kisomo cha Qur'an katika Sala hususan katika Salat Al Fajr ambamo ndio inatakiwa kirufushwe ndani yake.'**

Na suali linapokuja kuulizwa juu ya nani anaeshuhudia basi jibu hua ni Malaikat Rahman. Kwani amesema Abu Hurayrah kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Malaika wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* wanaowasimamia Bani Adam katika wakati wa Usiku hua ni wenye kubadilishana zamu na Malaika wa Mchana katika wakati wa Alfajir.'***(Imam Ibn Jarir)*

Hivyo anasema Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kua: **'Tukitafsiri Duluk na Ghasak basi tunaona kua zimaetajwa Nyakati tatu ambazo ni Wakati wa Adhuhuri, Wakati wa Magharibi na wakati wa Al Fajir. Hivyo hii inamaanisha kua Duluk ni wakati wa Sala ya Adh Dhuhr na Al Asr, na wakati wa Ghasaq hua ni wakati na Sala ya Maghrib na Sala ya Al Isha. Na hii inaonesha ruhusa ya ulazima wa kuchanganya Sala ya Adh Dhuhr na Al Asr, na Salat Al Maghrib na Al Ishaa. Lakini hata hivyo kuchanganya Sala katika Mji bila kua Safarini hua hairuhusiwi, ila huruhusiwa pale Unapokua Safarini, unapokua na dharura kama vile ya mvua au dharurah nyengine.'*(Mafatih Al Ghayb)*

Na Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Farra Al Baghawi Al Shafi.Amesema kua:'**Duluk maana yake hua ni kushuka kwa Jua na hivyo humaanisha Sala ya Adh Dhuhr ambaondio mtizamo unaoaminika zaidi kimaana na miongoni mwa Wanazuoni. Na hivyo Aya inajumuisha Sala ya Adhudhr na Al Asr na Ghasaq Al Layl kunamaanisha Sala ya Magharibi na Sala ya Isha na Kisomo cha Al Fajir hua iamaanisha Salat Al Fajr.'**

Ama kwa upande wa Imam Al Mubarrad basi yeye amesema kua: **'Duluk Al Shams maana yake hua ni kuanzia Adhuhuri hadi kuzama kwa Jua, kwa hivyo Adhuhr imeitwa kwa Jina hilo kwa sababu**

mwenye kulitizama Jua katika wakati huo hua ni mwenye kufinya Macho yake kutokana na ukali wa miale yake.

Ama kuhusiana na Ghasaq Al Layl basi hua ni kuonekana kwa Kiza cha Usiku, au ni katika wakati wa kiza cha Usiku. Kwani Usiku hua ni Giza linapozidi.'

Na amesema Imam Al Bayhaqi kua : **'Amesema Musa Ibn Uqba kua: 'Umar Ibn Abd Al Aziz alikua akichanganya' Salat Al Maghrib na Salat Isha pale inapokua inanyesha Mvua, na Said Ibn Musayyib, Urwah Ibn Zubaya, Abu Bakr Ibn Abd Rahman na Wanafiqh wa wakati huo walikua nao pamoja nao na hakuna aliewapinga juu ya hilo.'***(Sunan Al Kubra)*

Na Abd Rahman Ibn Harmalah amesema kua: **'Mimi nimemuona Said Ibn Musayyib akisali pamoja na Imam katika wakati ambao walikua wakichanganya Sala ya Maghribi na Isha katika usiku wa Mvua kubwa'***(Musannaf Imam Ibn Shaybah)*

Na Abu Mawdud Abd Al Azizi Ibn Abi Sulayman amesema kua: 'Mimi nilisaliSalat AlMaghrib na Salat Al Isha pamoja na Abu Bakr Ibn Muhammad na alikua akizichanganya katika Usiku wenye Mvua.' *(Musannaf Imam Ibn Shaybah)*

Na Imam Malik Ibn Aanas amesema kua: **'Salat Al Maghrib na Salat Al Isha hua zinachanganywa ndani ya Mji pale inapokua hakuna Mvua na na ikiwa kuna Matope na Kiza, na Mvua ikinyesha pia'***(Al Mudawwana)*

YALIYORUHUSIKA KATIKA ADHANA YA KUJUMUISHA SALA.

❖❖❖❖

Kwani tumeangalia kuhusiana na kuruhusika kuchanganya Sala kutokana na Dharurah, hivyo kuna baadhi yetu ambao wanaweza wakajiuliza suali lifuatalo: '**Jee kama inatokea Dharurah kama hio kwa mfano kama Mvua Nyingi, Theluji, Matope, Kimbunga, na hata pia Maradhi ya Kuambukiza kama ilivyokua katika wakati wa Korona Virus hivyo Kusali Nyumbani hua ni Salama zaidi kwaWaumini, hivyo Unapowadia Wakati wa Sala Muadhini ataadhini vipi?.'**

Naam...Juu ya hili pia basi Wanazuoni wanakubaliana kua katika Hali ya Dharurah kama hii basi maneno ya Adhana hua yanabadilika na hivyo baada ya Adhana kua ni yenye kuwaita Msikitini katika Ibada ya Sala na katika Mafanikio basi hua ni yenye kuwaamrisha Watu Kusali Majumbani mwao, kwa usalama wao.

Ambavyo ni kama alivyosema Imam Abu Daud na Imam Ahmad Ibn Hanbal katika Hadith ifuatayo: ''**Amesema Usamah Ibn Umayr *Radhi Allahu Anhu* kua:**

أَنَّ يَوْمَ حُنَيْنٍ كَانَ يَوْمَ مَطَرٍ، فَأَمَرَ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، مُنَادِيَهُ: أَنَّ الصَّلَاةَ فِي الرِّحَالِ

Katika Vita vya Hunayn kulikua na Mvua kubwa sana, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawanadia Watu Wasali ndani ya Mahema yao.'*(Sunnan Imam Abu Daud, Musnad Imam Ahmad)*

Na amesema Imam Al Bukhari kua:

أَلاَ صَلُّوا فِي الرِّحَالِ، ثُمَّ قَالَ: إِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَأْمُرُ المؤَذِّنَ إِذَا كَانَتْ لَيْلَةٌ ذَاتُ بَرْدٍ وَمَطَرٍ، يَقُولُ: أَلاَ صَلُّوا فِي الرِّحَالِ

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* aliadhini Katika Usiku Mmoja wa Baridi Kali na uliokua na Upepo Mkali sana, na kisha akasema katika Adhana hio maneno yafuatayo: '***Aalla Ssaluu Fi Rihalikum*** **- Salini Kwenye Makazi yenu.Na kisha akasema Abd Allah Ibn Umar** ***Radhi Allahu Anhu*** **kua:*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akimuamrisha Muadhini pale inapokua ni Usiku wa Baridi kali na Mvua kubwa kua aseme *Aalla Ssalu Fii Rihalikum* - Salini Katika Makazi yenu.'***(Sahih Bukhari na Muslim)***

Na anasema Imam Al Bukhari kua amesema Abd Allah Ibn Harith kua:

خَطَبَنَا ابْنُ عَبَّاسٍ فِي يَوْمٍ رَدْغٍ، فَلَمَّا بَلَغَ المؤَذِّنُ حَيَّ عَلَى الصَّلاَةِ، فَأَمَرَهُ أَنْ يُنَادِيَ الصَّلاَةُ فِي الرِّحَالِ

'Siku moja katika Siku ya Mvua Kubwa na iliyojaa Matope, basi Abd Allah Ibn Abbas ***Radhi Allahu Anhu*** **aliyoa Khutba mbele yetu na ulipowadia wakati wa Kuadhini basi akamuamrisha Muadhini Kuadhini na kumwambia:Utakapofika kwenye** ***Hayya aAla Al Salat basi sema Al Salatu Fii Al Rihalikum*** **- Kusali Ndani ni ya Makazi yenu.'***(Sahih Al Bukhari)*

Ambapo Imam Muslim pia ameinukuaa hadithi hii kwa kusema kua:

، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ الحَارِثِ ، عَنْ عَبْدِ اللهِ بْنِ عَبَّاسٍ ، أَنَّهُ قَالَ لِمُؤَذِّنِهِ فِي يَوْمٍ مَطِيرٍ : " إِذَا قُلْتَ : أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللهُ ، أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللهِ ، فَلَا تَقُلْ : حَيَّ عَلَى الصَّلَاةِ ، قُلْ : صَلُّوا فِي بُيُوتِكُمْ " ، قَالَ : فَكَأَنَّ النَّاسَ اسْتَنْكَرُوا ذَاكَ ، فَقَالَ: " أَتَعْجَبُونَ مِنْ ذَا ؟! ، قَدْ فَعَلَ ذَا مَنْ هُوَ خَيْرٌ مِنِّي ، إِنَّ الْجُمُعَةَ عَزْمَةٌ ، وَإِنِّي كَرِهْتُ أَنْ أُحْرِجَكُمْ ، فَتَمْشُوا فِي الطِّينِ وَالدَّحْضِ

Amesema Abd Allah Ibn Harith kua Abd Allah Ibn Abbas ***Radhi Allahu Anhu,*** **alimuamrisha Muadhini katika Siku moja ya Mvua Kali kwa Kumwambia:Utakaposema** ***Ashhadu An La Ilaha Illa Allah, Ashhadu An Na Muhammadan Rasul Allah,*** **basi baada yake usiseme:** ***'Hayya aAala Al Salah'*** **bali sema:** ***'Ssalu Fi Buyutikum!(*****Salini Majumbani Kwenu).**

Jambo hili liliwashangaza watu,na hivyo Abd Allah Ibn Abbas ***Radhi Allahu Anhu*** **akahoji kwa kusema: Inakuaje Mnashangazwa na Jambo hili?.**

Wakati M-bora zaidi yangu alifanya hivyo, Ndio kweli, Sala ya Ijumaa hua Ni Wajibu, lakini mimi sipendi kukuadhirisheni nyinyi kwa kukupelekeeni kutembea Matopeni na Kujichafua.'*(Sahih Muslim)*

Ambapo anasema *Mujaddid Ad Din* Al Hafidh Imam Ibn Hajar Al Asqallani kua : '**Ni jambo lililowazi kabisa kua Kauli hio iliyoongezewa ilitamkwa baada ya kumalizika Adhana.'***(Fat-h Al Barr)*

Ambapo amesema Al Hafidh Imam Abu Fadhl Zayn Ad Din Abd Rahim Ibn Al Husayn Al Iraqi Al Shafii kua: '**Maneno yasemayo Salini Ndani ya majumba yenu' ni yenye kupingana na maneno yasemayo Njooni Katika Sala.Hivyo Katika hali kama hii basi Hua si Sahih kwa Muadhini kusema Njooni Katika Sala na kisha kusema Msije bali Salini Majumbani mwenu.'***(Tarh Al Tathrib)*

Na akasema Imam Ibn Hajar Al Asqallani pia kua: '**Inakubalika kutumia maneno yote mawili, bila ya kulazimisha kile kinachosemwa ndani ya Adhana.Hivyo katika hali kama hii basi hua kuna Khiari, kutokana na amrisho la Kusali Majumbani, na kuenda Msikitini, hivyo atakaetaka Kusali Nyumbani atasali Nyumbani na kukamilisha Malipo ya Jamaa, na atakaeshindwa kutokana na Ugumu wa hali ya mazingira basi atasali Nyumban**i.'*(Fat-h Al Barr)*

Na pia amesema Nuayl Ibn Al Nahham *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Muadhini wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiadhini katika Usiku wa Mvua kubwa wakati tulipokua Safarini kwa kusema:*Hayya Aala Al Salaah, Hayya Aala Al Falah Sallu fi Rihalikum*.'** *(Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo katika Mawsuat Al Fiqhiyyah Al Quwaytiyyah imeelezwa pia kua: '**Inaruhusika kwa Muadhini Kuadhini kwa kuamrisha *Sallu Fi Buyutikum* (Salini katika Majumba yenu) pale inapokua Kuna Mvua kubwa, Kuna Radi zinazopiga Sana, Kuna Baridi Kali na Hali nyengine za Mazingira kama hayo.'**

Ambapo kwa upande wa Shaykh Al Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi basi yeye amesema kuhusiana na Hadith mbili hizi kua: '**Katika Hadith ya Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* basi yeye aliamrisha Salini Majumbani mwenu, Mwishoni mwa Adhana kamilifu**. **Na katika Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye aliesema kua Salini Majumbani Mwenu badala ya maneno Njooni Katika Sala, Njooni katika Mafanikio. Hivyo hali zote mbili hizi hua inakubalika. Kama alivyosema Imam Al Shafii *Rahima humu Allahu* katika Kitabu chake cha Al Umm katika Mlango wa Adhaana.**

Na pia Wengi Miongoni mwa Wanazuoni wetu Wamemfuata Imam Al Shafii katika Mtizamo huuYaani inakubalika Kusema Sallu aAala Buyutikum baada ya Adhana na pia ndani ya Adhana, na hii ni kwa sababu hali zote mbili zimethibitishwa na Sunnah.

Lakini hata hivyo kusema Maneno hayo baada ya Adhana hua ni bora zaidi, ili Mpangilio wa maneno ya Adhana usibadilike, bali ubakie kama ulivyo katika Uasili wake.*(Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Muflih Al Hanbal basi yeye anasema baada ya kunukuu Hadith zote mbili hizi za Abd Allah Ibn Abbas na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum* kua: **'Hadith hizi zinainesha kua Mtu anaweza akatumia Njia atakyoipenda baina ya njia mbili hizo'***(Al Furu)*

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi amesema tena katika Rawdha Talibin kua:**'Katika Hali hii basi Hua ni Sunna kusema Sallu Fii Buyutikum baada ya Adhana, na hivyo hata kama Mtu atataka kuyasema ndani ya Adhana. Basi hua inatakiwa ayaseme baada ya Al Haila'ah yàani baada ya Hayya Al Salaa au Hayya Ala Al Falaa na hua ana tatizo.'** *(Rawdhah Talibin)*

YALIYORUHUSIKA KUKATISHA SALA JUU YAKE.

❖❖❖❖

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَلَا تُبۡطِلُوٓاْ أَعۡمَٰلَكُمۡ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo ateeAAoo Allaha waateeAAoo alrrasoola wala tubtiloo aAAmalakum *(Surat Muhammad 47:33)*

Tafsir: ***Enyi Wale ambao Mlioamini Mtiini Allah na Mtiini Mtume Na Wala Msizibatilishe Amali zenu.***

Naam..Hii ni Aya ambayo tumeshaiangalia hapo Kabla na kama inavyotuonesha kua ndani yake kua kuna Maamrisho Mawili Muhimu Sana.

Ambayo ni Amrisho la Kumtii *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Kumtii *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Kutekeleza Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Kuachana na Makatazo yake. Na kisha Ikaamrisha kwa kukataza kutobatilisha Amali zetu Njema.

Ambapo anasema Imam Abu Aliyyah kua amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walikua wakiamini kua kutokana nabkua Amali njema zao zilizofanywa katika Wakati wa Ujahiliyah hazitokubaliwa, basi bila ya shaka hata Maovu yao baada ya kusilimu hayatowaathiri, hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* aliposhusha aya hii kuhusiana na kupukutika kwa Amali njema.'**

Ambapo amesema Imam Ibn Jarir At Tabari kua:**'Amesema Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi amesema kuhusiana na Aya hii kua inamaanisha kua: Yeyote yule miongoni mwenu basi ajitahidi atakavyoweza kutoziangamiza Amali njema zake kwa Kufanya Dhambi baada ya Kufanya mema yake.'**

Na Mujaddid Ad Din, Sultan Al Mutakallimin, Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii anasema kua:**'Maneno ya Aya hii yanamaanisha kua Msimshirikishe *Allah Subhanah wa Ta'ala* baada ya Kusilimu kwenu, Kwani kama mkifanya hivyo basi Aamali zenu Njema zote mlizofanya hapo kabla zitabatilika.'**

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika sehemu nyengine ndani ya Kitabu chake kua:

﴿ وَلَقَدۡ أُوحِيَ إِلَيۡكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكَ لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾

Walaqad oohiya ilayka wa-ila alladheena min qablika la-in ashrakta layahbatanna AAamaluka walatakoonanna mina alkhasireena.*(Surat Az Zumar 39:65)*

Tafsir: ***Kwa Hakika Umeshushwa Wahyi Kwako(Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Na Kwa Wale wengineo Kabla yakoKua Kama Ukimshirikisha Allah basi Tutazibatilisha Aamali zakoNa Kwa Hakika Utakua Miongoni mwa Waliokula Hasara****.*

Na akasema Jarrah Allah, Sultan Al Balagha Imam Abu Qasim Al Zamakhshari Al Hanafi kua:**'Abd**

Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akisema kua: Dhambi Kubwa hua ni zenye kupelekea kuangamia kwa Amali njema za Mtu, lakini kutokana na maneno ya aya ifuatayo:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغۡفِرُ أَن يُشۡرَكَ بِهِۦ وَيَغۡفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُۚ وَمَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱفۡتَرَىٰٓ إِثۡمًا عَظِيمًا﴾

Inna Allaha la yaghfiru an yushraka bihi wayaghfiru ma doona dhalika liman yashao waman yushrik biAllahi faqadi iftara ithman AAa*dh*eeman*(*Surat An Nisaa 4:48)***

Tafsir:Hakika ya Allah HasamehеKushirikishwa NaeNa Husamehe Dhambi Nyengine isipokua Hio (Ya Ushirikina)Kwa Yule AmtakaeNa Mwenye Kumshirikisha AllahBasi kwa Hakika huani mwenye Kuvumbua Dhambi Kubwa Sana.

Naam..Imam Al Zamakhshari anaendelea kusema kua: **‘Baada ya kushuka Aya hii, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akabadilisha Mtizamo wake na kusema: Khofu ya Adhabu Kali Inawahusu wale ambao ni wenye Kufanya Dhambi kubwa na Matumaini ya kusamehewa yanawahusu wale ambao hawakufanya Madhambi Makubwa.’***(Tafsir Al Kashshaf-Imam Al Zamakhshari)*

Ambapo katika aya nyengine basi *Allah Subhanah wa Ta’ala* amesema kua:

﴿قُلۡ يَٰعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ أَسۡرَفُواْ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمۡ لَا تَقۡنَطُواْ مِن رَّحۡمَةِ ٱللَّهِۚ إِنَّ ٱللَّهَ يَغۡفِرُ ٱلذُّنُوبَ جَمِيعًاۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلۡغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ﴾

Qul ya AAibadiya allatheena asrafoo AAala anfusihim la taqnatoo min rahmati Allahi inna Allaha yaghfiru aldhdhunooba jameeAAan innahu huwa alghafooru alrraheemu*(Surat Az Zumar 39:53)*

Tafsir: **Waambie*(Ewe Rasul Allah Salallahu Alayahi wa Salam)* Enyi waja wangu wale ambao waliofanya Israfu dhidi ya Nafsi zao, msivunjike Moyo na Rehma za Allah, kwani kwa hakika Allah ni mwenye kusamehe Dhambi zote, Hakika yeye ni Msamehevu na ni Mwingi wa Rehema.**

Kwa sababu *Allah Subahanh wa Ta’ala* ni mwenye kujua juu ya kila kitu kuhusaina na Viumbe wake, hivyo ni mwenye kupenda kuwasaidia Waja wake kwa kuwanyooshea Mkono kuwavuta kwa ajili ya kuwaingiza ndani ya Rehma zake, na hivyo hua si mwenye kupenda kuwakamata na kuwaingiza kwenye adhabu zake kabla ya kuwapa fursa ya kurudi kwake.

Hivyo Ibn Adam anaweza akatumbukiwa na kuzama ndani ya dhambi kubwa sana, kiasi ya kua akaona kua hakuna njia ya kutoka nje yake, ambapo hata hivyo hata kama atafiia katika hali kama hio basi hua hatakiwi kuvunjika Moyo kutokana na Rehma za Mola wake, na ndio maana *Allah Subhanah wa Ta’ala* akashusha Aya hii.

Ambapo wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Karne za mwanzoni za Uislam wameitafsiri aya hii kua ni yenye kuhusiana na wale Wasiokua Waislam na kisha wakawa ni wenye kutaka kungia ndani ya Dini ya Kiislam na kufanya Mema basi kua watasamaehewa dhambi zao zote zilizotangulia hapo kabla.

Kama vile ilivyoelezewa katika vitabu viwili vya Hadith Sahih vya Sahih Bukhari na Sahih Muslimkatika hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ، حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ أَبِي عَدِيٍّ، عَنْ شُعْبَةَ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ أَبِي الصِّدِّيقِ النَّاجِيِّ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ ـ رضى الله عنه ـ عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَ "كَانَ فِي بَنِي إِسْرَائِيلَ رَجُلٌ قَتَلَ تِسْعَةً وَتِسْعِينَ إِنْسَانًا ثُمَّ خَرَجَ يَسْأَلُ، فَأَتَى رَاهِبًا فَسَأَلَهُ، فَقَالَ لَهُ هَلْ مِنْ تَوْبَةٍ قَالَ لاَ. فَقَتَلَهُ، فَجَعَلَ يَسْأَلُ، فَقَالَ لَهُ رَجُلٌ ائْتِ قَرْيَةَ كَذَا وَكَذَا. فَأَدْرَكَهُ الْمَوْتُ فَنَاءَ بِصَدْرِهِ نَحْوَهَا، فَاخْتَصَمَتْ فِيهِ مَلاَئِكَةُ الرَّحْمَةِ وَمَلاَئِكَةُ الْعَذَابِ، فَأَوْحَى اللَّهُ إِلَى هَذِهِ أَنْ تَقَرَّبِي. وَأَوْحَى اللَّهُ إِلَى هَذِهِ أَنْ تَبَاعَدِي. وَقَالَ قِيسُوا مَا بَيْنَهُمَا. فَوُجِدَ إِلَى هَذِهِ أَقْرَبُ بِشِبْرٍ، فَغُفِرَ لَهُ ".

Amesema Muhammad Ibn Bashar kua amesema Muhammad Ibn Abi Addiy kua amesema Shuaybah kua amesema Qatadah kua aemsema AbiSiddiq An Najji kua amesema Abu Said Al Khdhri *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna Mtu miongoni mwa watu wa Bani Israil ambae alikua ameua Watu 99. Hivyo akatoka na kutaka kuulizia kama toba yake itakubaliwa ama la. Akamfuata Kuhani na kumuuliza kama Toba yake itakubaliwa, na Kuhani huyo akasema La. Hivyo Mtu huyo akamuua Kuhani huyo.

Na kisha akaendelea kuuliza hadi akashauriwa kua aende katika Kijiji ambacho akae pamoja na watu wake na atakubaliwa Toba yake. Hivyo akaelekea kwenye kijiji hicho lakini njiani akakutana na Mauti yake. Na wakati anafariki basi alikua amegeukia kifua chake upande uliopo kijiji hicho. Hivyo Malaika wa Rehma na Malika wa Adhabu wakawa wanagobaniana nae, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akakiamrisha Kijiji alichokua anakielekea kukaribia Maiti ya mtu huyo na kile kijiji alichotoka kusogea mbali nae. Na kisha akawaamrisha Malaika hao kupima masafa baina ya Mwili wake mtu huyo na Vijiji viwili hivyo, na ikaonekna kua Mwili wake ulikua karibu zaidi na alikukua anaelekea kwa masafa ya Pima moja, na hivyo akawa ni mwenye kusamehewa.*(Sahih Bukhari)***

Na pia hadithi hii imesimuliwa katika Sahih Muslim kama ifuatavyo:

وعن أبي سعيد سعد بن مالك بن سنان الخدري رضي الله عنه أن نبي الله صلى الله عليه وسلم قال: "كان فيمن كان قبلكم رجل قتل تسعة وتسعين نفساً، فسأل عن أعلم أهل الأرض، فدل على راهب، فأتاه فقال: إنه قتل تسعه وتسعين نفساً، فهل له من توبة؟ فقال: لا، فقتله فكمل به مائةً، ثم سأل عن أعلم أهل الأرض، فدل على رجل عالم فقال: إنه قتل مائة نفس فهل له من توبة؟ فقال: نعم، ومن يحول بينه وبين التوبة؟ انطلق إلى أرض كذا وكذا، فإن بها أناساً يعبدون الله تعالى فاعبد الله معهم، ولا ترجع إلى أرضك فإنها أرض سوءٍ، فانطلق حتى إذا نصف الطريق أتاه الموت، فاختصمت فيه ملائكة الرحمة وملائكة العذاب. فقالت ملائكة الرحمة: جاء تائبا مقبلا بقلبه إلى الله تعالى، وقالت ملائكة العذاب: إنه لم يعمل خيرا قط، فأتاهم ملك في صورة آدمي فجعلوه بينهم- أي حكماً-

فقال: قيسوا ما بين الأرضين فإلى أيتهما كان أدنى فهو له، فقاسوا فوجدوه أدنى إلى الأرض التي أراد، فقبضته ملائكة الرحمة" ((متفق عليه)).

‘Amesema Abu Said Said Ibn Malik Ibn Sinan Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kulikua na Mtu miongoni mwa watu wa kabla yenu ambae aliua watu mia tisa na tisisni na tisa. Na kisha akauilizia kuhusiana na Mtu mwenye Ilm kubwa zaidi kuliko wote Duniani, na hivyo akaelekezwa kwa Kuhani mmoja. Na hivyo akafunga Safari kuelekea kwa Kuhani huyo na alipofika akamuulizia kuhusiana na kama kuna Toba kutokna na aliyoyafanya.

Hivyo Kuhani huyo akasema: ‘La!’ na hivyo Mtu hu akamuua Kuhani huyo na kua ni mwenye kutimiza idadi ya watu 100 aliowaua’

Na kisha akaulizia kuhusiana na Mtu mwenye kujua zaidi miongoni mwa Watuwalioko Duniani. Na hivyo akaelekezwa kwa Mmoja kati ya Wanazuoni, na akaelekea kwa Mwanazuoni huyo, na alipofika akamwambia: ‘Hakika mimi ni Mtu ambae nimeua Watu 100, hivi jee unadhani kuna kuna uwezo wa mimi kuweza kusamehewe na *Allah Subhanah wa Ta’ala*?’

Yule Mwanazuoni akasema: ‘Naam bila ya Shaka! Hivi unafikiria wewe ni nani anaeweza kuingilia kati baina yako na usamehevu wa Mola wako? Hivyo nenda katika Kijiji Fulani ambacho kina watu ambao ni wenye kujitolea kwa ajili ya kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta’ala* tu. Na kisha bakia hukohuko pamoja nao ili nawe ujitolee kwa ajili ya kuuabudu *Allah Subhanah wa Ta’ala* na wala usirudi kwenye kwenye Ardhi uliyotoka ya watu ambao hawana wema ndani yake.’

Hivyo Mtu huyyo akaanza safari ya kuelekea kwenye kijiji hicho alichoelekezwa, hadi akafikia masafa ya kua ameshatembea Nusu ya safari yake. Na kifo kikamkuta ndani yake. Hivyo Malaika wa Rehma na Malaika wa Adhabu wakaanza kugombaniana juu ya Roho yake mtu huyo ambapo Malaika wa Rehma wakasema: ‘Mtu huyu amefunga Safari kwa ajili ya kutubu, huku Moyo wake ukiwa umeelekea kwa ajili ya kurudi kwa *Allah Subhanah wa Ta’ala.’*

Na Malaika wa Adhabu wakawa ni wenye kusema: ‘La Hakika ya Mtu huyu hakua ni mwee kufanya Jema hata moja katika uhai wake.’

Na mara akatokea Malaika katika umbile la Ibn Adam nan a hivyo Malaika wakamchagua kua ni mwenye kutatua mgogoro huo baina yao. Na Malaika huyyo akasema: ‘Pimeni Masafa ya sehemu mili kutoka hapa yalipomkuta Mauti, na kisha mtamhukumu kulingana na Ukaribu wa baina ya sehemu mbili hizo’ na Malaika walipopima wakakuta kua Mtu huyyo alikua amekaribia zaidi kule anakoelekea kwa zaidi ya urefu pima moja. Hivyo Malaika wa Rehma wakaichukua Roho yake Mtu huyo.’*(Sahih Bukhari na Muslim –Mutaffaq Alayh)*

Hivyo Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu a*mesema kuhusiana na Ayah ii kua: ‘**Aya hii inamaanisha kua Kwa kila Muislam ambae amefanya dhambi iwe kubwa au ndogo basi atakua ni mwenye kusamehewa dhambi zake kama akitubu’.**

Kwa hivyo ayah hii inamhusu kila Mtu, kwani kwa upande wa Muislam kama akifanya Dhambia iwe kubwa ama ndogo, na kisha akarutdi kwa Mola wake kwa kutubu basi atamkuta *Allah Subhanah wa Ta’ala* ni mwenye kumsubiri na kumpokea kwa huruma, mapenzi na usamehevu mkubwa Mja wake huyo na kama Mtu huyo si Muislam na ameshafanya madhambi mengi sana lakini akaamua kuingia

kwenye Uislam atamkuta *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni mwenye kumsubiri na kumpokea kwa huruma, mapenzi na usamehevu mkubwa Mja wake huyo pia.

Kwani bila kurudi kwake na kutubu basi itakua hakuna kunusirka kutokana na Adhabu zake na haitowezekana kupata rehma zake kama alivyosema katika aya ifuatayo:

﴿وَأَنِيبُوٓاْ إِلَىٰ رَبِّكُمۡ وَأَسۡلِمُواْ لَهُۥ مِن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَكُمُ ٱلۡعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ﴾

Waaneeboo il<u>a</u> rabbikum waaslimoo lahu min qabli an ya/tiyakumu alAAa<u>dha</u>bu thumma l<u>a</u> tun<u>s</u>aroona.*(Surat az zumar 39:54)*

Tafsir: ***Na rudini kwa kutubu kwa Mola wenu na Mjisalimishe kwake kabla hajakupeni Adhabu na kisha hamtonusurika.***

Kwani ni wale tu wenye kurudi kwa Mola wao na kumtii basi ndio watakaopata urahisi wa juu ya kila kitu kama zilivyoahidi aya kwa kusema kua:

﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجٗا ۝ وَيَرۡزُقۡهُ مِنۡ حَيۡثُ لَا يَحۡتَسِبُ وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓ إِنَّ ٱللَّهَ بَٰلِغُ أَمۡرِهِۦ قَدۡ جَعَلَ ٱللَّهُ لِكُلِّ شَيۡءٖ قَدۡرٗا﴾

Waman yattaqi All<u>a</u>ha yajAAal lahu makhraj<u>a</u>n; Wayarzuqhu min <u>h</u>aythu l<u>a</u> ya<u>h</u>tasibu waman yatawakkal AAal<u>a</u> All<u>a</u>hi fahuwa <u>h</u>asbuhu inna All<u>a</u>ha b<u>a</u>lighu amrihi qad jaAAala All<u>a</u>hu likulli shay-in qadr<u>a</u>n*(Surat At Talaq 65:2-3)***

Tafsir: ***Na Yeyote yule atakaemuogopa na kumtii Allah Subhanah wa Ta'ala, basi Allah Subhanah wa Ta'ala atamjaalia njia ya kutokea katika kila lililogumu. Na Atamruzuku kutokana na vyanzo asivyovitegemea, Na yeyote yule atakaemtegemea kikamilifu Allah Subhanah wa Taala, basi Allah Subhana wa Ta'ala atatamtosheleza.Kwani kwa Hakika Allah Subhanah wa Ta'alaaAmekamilisha Jambo Lake, Hakika Allah Subhanah wa Ta'ala mejaalia kila kitu kua na makadirio yake.***

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: **'Amesema Ra*sul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Naapa Mimi kwayule ambae Uhai wangu uko ndani ya mikono yake kua Hata kama Nyinyi Mkifanya Dhambi hadi kufikia hali ya kua Dhambi zenu zikajaa baina ya Mbingu na Ardhi na kisha mkaomba Msamaha kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Bila ya Shaka Atakusameheni. Na Naapa kwa yule ambae Uhai wangu umo ndaniya mikono yake kua, hata kama nyinyi mngekua hamfanyi dhambi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* angewaleta watu badala yenu ambao wangefanya Dhambi na kisha kuomba Msamaha wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Yeye Angewasamehe.''**

Ambapo amesema Imam Ibn Hajar Al Haythami Al Makki Al Shafii kua: **'Hadith hii ni yenye Sanad iliyo sahih'**

Na Imam Muslim anahadith isemayo kua:

حَدَّثَنِي مُحَمَّدُ بْنُ رَافِعٍ، حَدَّثَنَا عَبْدُ الرَّزَّاقِ، أَخْبَرَنَا مَعْمَرٌ، عَنْ جَعْفَرٍ الْجَزَرِيِّ، عَنْ يَزِيدَ بْنِ الأَصَمِّ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوْ لَمْ تُذْنِبُوا لَذَهَبَ اللَّهُ بِكُمْ وَلَجَاءَ بِقَوْمٍ يُذْنِبُونَ فَيَسْتَغْفِرُونَ اللَّهَ فَيَغْفِرُ لَهُمْ "

Amesema Muhamamd Ibn Rafii kua amesema Abd Razzak Maamaru kua amesema Jafar Al Jazari kua amesema Yazi Ibn Asami kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* amesema kua: 'Hata kama nyinyi mngekua hamfanyia dhambi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* angewaleta watu badala yenu ambao wangefanya Dhambi na kisha kuomba Msamaha wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Yeye Atawasamehe.'

Na amesema Ayub Al Ansari *Radhi Allahu Anh*u wakati alipokua Kitandani katika mwishoni mwa uhai wake kua: **'Kwa Hakika mimi kuna kitu nimekificha kutokana nanyi, ambacho ni kua nimemsikia *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* akisema kua: 'Hata kama nyinyi mngekua hamfanyia dhambi basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* angewaleta watu badala yenu ambao wangefanya Dhambi na kisha kuomba Msamaha wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Yeye Atawasamehe.''**

Na amesema Imam At Tirmidhii kua:

عَنْ أَنَسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ ، قَالَ : سَمِعْتُ رَسُولَ اللهِ صَلَّى الله عَلَيْهِ وَ سَلَّمَ ، يَقُولُ : قَالَ اللهُ تَعَالَى : يَا ابْنَ ادَمَ ، إِنَّكَ مَا دَعَوْتَنِي وَرَجَوْتَنِي ، غَفَرْتُ لَكَ عَلَى مَا كَانَ مِنْكَ وَلَا أُبالِي . يا ابْنَ ادَمَ :لَوْ بَلَغَتْ ذُنُوبُكَ عَنانَ السَّماءِ ثُمَّ اسْتَغْفَرْتَنِي ، غَفَرْتُ لَكَ . يَا ابْنَ ادَمَ : إِنَّكَ لَوْ أَتَيْتَنِي بِقُرَابِ الأَرْضِ خَطَايا ثُمَّ لَقِيتَنِي لَا تُشْرِكُ بِي شَيْأً ، لَأَتَيْتُكَ بِقُرَابِها مَغْفِرَةً رواهُ الترمذي (وكذلك أحمد) وسنده حسن

Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Nimemsikia mimi *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* akisema kua: Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: 'Enyi Ibn Adam Kila Mkiendelea kuniomba Msamaha basi hakika mimi nitakusameheni kwa yale mliyoyafanya, na sitojali, Enyi Ibn Adam hata kama Madhambi yenu yatafikia hadi kwenye Mbingu kwa wingi wake na kisha Mkaniomba Msamaha, Basi mimi nitakusameheni, Enyi Ibn Adam hata kama mkija mbele yangu na Dhambi zitakazofikia ukubwa wa Dunia bila ya kunishirikisha' basi Nami nitakupeni msamaha Kwa Ukubwa wa Mithili yake.*(Hadith Al Quds, Imam At Tirmidhi, Imam Ahmad Ibn Hanbal)***

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua:'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

إِنَّ الشَّيْطَانَ قَالَ وَعِزَّتِكَ يَا رَبِّ لَا أَبْرَحُ أُغْوِي عِبَادَكَ مَا دَامَتْ أَرْوَاحُهُمْ فِي أَجْسَادِهِمْ قَالَ الرَّبُّ وَعِزَّتِي وَجَلَالِي لَا أَزَالُ أَغْفِرُ لَهُمْ مَا اسْتَغْفَرُونِي

Hakika Ya Shaytan alisema kumwambia *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua: **'Naapa kwa uwezo wako kua Wakati Roho za Ibn Adam zimo ndani ya Miili yao basi Mimi nitaendelea kuwapotosha tu.**

Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema kua: 'Kwa Uwezona Nguvu zangu basi Kila wakiendelea kuniomba Msamaha basi Na mimi Nitaendelea Kuwasamehe''

Na amesema Imam Ibn Majah kua:'**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

طُوبَى لِمَنْ وَجَدَ فِي صَحِيفَتِهِ اسْتِغْفَارًا كَثِيرًا

Atapendezeshwa yule ambae atakuta katika kitabu chake cha Malipo, Istighfar Nyingi sana.*(Sunnan Ibn Majah)*

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pia kua:

مَنْ أَحَبَّ أَنْ تَسُرَّهُ صَحِيفَتُهُ فَلْيُكْثِرْ فِيهَا مِنَ الِاسْتِغْفَارِ

'Yeyote atakaependa kua ni mwenye kupendezeshwana Kitabu chake cha hesabu basi na Azidishe kufanya Istighfar.*(Shuy'ab Al Iman)*

Na amesema Abu Bakr As Siddiq *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi***

مَا مِنْ رَجُلٍ يُذْنِبُ ذَنْبًا ثُمَّ يَقُومُ فَيَتَطَهَّرُ ثُمَّ يُصَلِّي ثُمَّ يَسْتَغْفِرُ اللَّهَ إِلَّا غَفَرَ اللَّهُ لَهُ

Hakuna Mtu atakaefanya Dhambi, na kisha akajitoharisha kwa Udhu na kisha akasali na akamuomba msamaha *Allah Subhana wa Ta'ala* isipokua *Allah Subhanah wa Ta'ala* humsamehe Mtu huyo.

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasoma aya ifuatayo:

﴿وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ وَمَن يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ وَلَمْ يُصِرُّوا عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ يَعْلَمُونَ﴾

Waallad<u>dh</u>eena i<u>tha</u> faAAaloo f<u>ah</u>ishatan aw *<u>dh</u>*alamoo anfusahum <u>dh</u>akaroo All<u>a</u>ha faistaghfaroo li<u>dh</u>unoobihim waman yaghfiru al<u>dhdh</u>unooba ill<u>a</u> All<u>a</u>hu walam yu<u>s</u>irroo AAal<u>a</u> m<u>a</u> faAAaloo wahum yaAAlamoona*(*SuratAl Imran 3:135)*

Tafsir: ***Na kwa walea ambao ikiwa wamefanya mambo maovu au wakajidhulumu Nafsi zao, na kisha wakamkumbuka Allah Subhanah wa Ta'ala na kumuomba Msamaha kwa maovu yao, basi ninani anaesamehe dhambi zaidi ya Allah Suhanah wa Ta'ala? Na kisha wakawa si wenye kudumu katika waliyoyafnya wakati wakijua.*** *(Imam At Tirmidhi)*

Na amesema** Zayd Ibn Harith Radhi Allahu Anhu* kua : **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam

مَنْ قَالَ أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ الْعَظِيمَ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيَّ الْقَيُّومَ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ غُفِرَ لَهُ وَإِنْ كَانَ فَرَّ مِنْ الزَّحْفِ

Atakaesema katika Dua yake *Astaghfir Allah Al Ladhii La Ilaha Illa Huwa Al Hayyu Al Qayyum Wa Atubu Ilayhi basi Allah Subhanah wa Ta'ala* atamsamehe Dhami zake hata ama alikua ni mwenye kukimbia kutka katika uwanja wa vita vya Jihad.*(Imam At Tirmdhi)*

Na Al Baraa aliambiwa kua: **'Ewe Abu Umarah, hivi jee maana ya aya isemayo kua'**

﴿وَأَنفِقُواْ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَلاَ تُلْقُواْ بِأَيْدِيكُمْ إِلَى ٱلتَّهْلُكَةِ وَأَحْسِنُوٓاْ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُحْسِنِينَ﴾

Waanfiqoo fee sabeeli Allahi wala tulqoo bi-aydeekum ila alttahlukati waahsinoo inna Allaha yuhibbu almuhsineena*(Surat Al Baqara 2:195)*

*Tafsir: **Na tumieni kwa ajili ya njia ya Allah Subhanah wa Ta'ala na wala msijitupe kwa mikono yenu kwenye maangamizi na fanyeni Mema kwani kwa Hakika Allah Subhanah wa Ta'ala nimwenye kuwapenda wenye kufanya Mema.***

Ni kuhusiana na Mtu ambae anakutana na adu yake katika uwanja wa vita na kisha akapigana hadi akafariki?'

Ambapo al Baraa *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'La! Bali hii maana yake ni kua Pale Mtu anapofanya Dhambi na kisha kawa nimwenye kusema kutokana na hili basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hatonisamehe'*(Shuab Al Iman)*

Na baada ya kuangalia maana za Aya kulingana na Mitizamo ya wanazuoni Tofauti basi tunaona kua lengo Kuu kabisa la aya hii inayokataza kubatilisha Amali zetu ni kutuamrisha kua Kimsingi Kila Amali itakayoanzwa kufanywa na Ibn Adam kwa ajili ya Mola wake, basi haitakiwi Kukatishwa wala Kubatilishwa.

Na ingawa Aya inatuarifu hivyo lakini pia kuna Hukmu inayotokana na Kanuni ya Msingi wa Fiqh isemayo kua

الضَّرُورَةُ تُبِيحُ االمِحْظُورَاتِ

Dharurah Hua ni Yenye Kuruhusu kile kilichokatazwa. Hivyo basi Haitakiwi kubatilisha Amali Njema isipokua kwa Dharurah maalum.

Na miongoni mwa Mifano hai iliyomo nfani ya Sunna Za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Kukatisha Ibada ya Sala ni kama ilivyosema Hadith ifuatayo:

أَخْبَرَنَا أَبُو عَبْدِ اللَّهِ، قَالَ: ثنا يُوسُفُ، قَالَ: حَدَّثَنِي أَبِي، قَالَ: النَّرْسِيُّ، قَالَ: حَدَّثَنَا عُبَيْدُ اللَّهِ بْنُ مُوسَى الْعَبْسِيُّ، قَالَ: ثنا شَيْبَانُ، عَنْ إِبْرَاهِيمَ بْنِ طَهْمَانَ، عَنْ هِشَامٍ الدَّسْتَوَائِيِّ، عَنْ يَحْيَى بْنِ أَبِي

كَثِيرٍ، عَنْ ضَمْضَمِ بْنِ جَوْسٍ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: اقْتُلُوا الأَسْوَدَيْنِ فِي الصَّلاةِ الْحَيَّةَ وَالْعَقْرَبَ

Amesema Abu Abd Allah kua amesema Yusuf kua amesema Baba Yangu kua amesema An Nasry kua amesema Ubayd Allah Ibn Musa kua amesema Shayban kua amesema Ibrahim Ibn Tahman kua amesema Hisham Al Dastawi kua amesema Yahya Ibn Abi Kathiri kua amesema Damdam Ibn Jaws kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:'Ueni Al Aswadayni (Vitu viwili vyeusi) ndani ya Sala zenu, Nyoka na Nge.'*(Imam Abu Daud,Imam Tirmidhi Imam Nasai, Imam Ahmad)***

Naam..kama tunavyojua kua kati ya Makusudio ya Sharia za Allah Subhanah wa Ta'ala hua ni Kuhifadhi Uhai wa Ibn Adam.Kwa maana hio basi daima Uhai na Uzima wa Ibn Adam hua unapewa Kipaumbele zaidi kuliko Uhai au Uzima wa Ibada husika.Ndio maana ikaamrishwa kua Mgonjwa Asifunge, asieweza kusimam basi Asali Akiaa amekaa, na asieweza kukaa Alale n.k.

Hivyo tunapoyaangalia Maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Hadith hii ambayo hua ni Sunnah ya Kauli, basi tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha Kuwaua Wadudu wawili hawa hata kama Mtu yumo ndani ya Sala.Na hii ni kwa Sababu Wadudu wawili hawa ni wenye kuweza Kuhatarisha Maisha ya Mtu anaesali au Mwengineo aliekua karibu yake.

Ambapo Amrisho hili linaweza likatekelezeka katika Njia mbili zifuatazo:**Njia ya kwanza ni ya Kumpiga Mdudu husika kwa Vipigo visivyozidi Vitatu na kumuua ambapo hii hua ni njia isiyopeleea Kubatilika kwa Salam.**

Na Njia ya pili hua ni Kupiga kwa zaidi ya Mara tatu ambako kutapelekea kubatilisha Sala husika, ambapo hua kunaruhusika.

Na bila ya shaka hapa hua inategemea na hali na mazingira husika, kwani unaweza ukapiga mara tatu na ukafanikisha, na ukaendelea na Sala, na unaweza ukapiga Mara tatu ukawa hukufanikisha na hivyo kukubidi kupiga zaidi ya mara tatu na hivyo baada kupatikana usalama na Sala kubatilika basi utaanza upya kusali tena Sala yako.

Ambapo tunapozungumzia kuhusiana na maana ya Al Aswadayni yaani vitu viwili Vyeusi basi tunaona kua Neno A*l Aswadayni* limetumika katika Sunnah za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumaanisha zaidi ya maana moja.

Kwani neno hili *Al Aswadayn hutumika kumaanisha* **Tende na Maji, katika Kutilia Mkazo Rangi ya Weusi wa Kawaida wa Tende, na Maji ambayo hayana Rangi, Kama ilivyosemwa katika Hadith na Aisha*Radhi Allahu Anha* kua:Sisi tulikua Tukiangalia Muandamo wa Mwezi Mara Tatu ndani ya Miezi Miwili, na hakuna Moto uliowashwa kwenye Nyumba ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.***

Walipoulizwa Aisha*Radhi Allahu Anha*walikua wanakula nini basi akajibu: 'Al Aswadayni Tende na Maji'.

Lakini Maana hii sio iliyokusudiwa kwenye Hadith hii,kwa sababu Al Aswadayn humaanisha pia Wadudu wawili ambao ni Nyoka na Nge.

Na amesema Imam Al Jawhari pia kua: **'Kuna Watu walimtembelea Muzabid Al Madani nae akawaambia kua: 'Hmna chochote kwa ajili yangu isipokua Al Aswadayn' na hivyo watu hao wakasema: 'Unaamisha Tende na Maji?' ambapo nae akasema: 'La nnamaanisha Joto na Usiku''***(Al Sahah)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Asmai, Imam Al Ahmar ,Imam Ibn Al Kalbi na wengine basi wao wanasema kua: **'Kusema kwake Aisha *Radhi Allahu Anha* 'Al Aswadayn' ambapo weusi ha ni wa Tende tu na wala si kwa ajili ya Maji kunamaanisha kuelezea vitu viwili kwa kupitia katika sifa ya kitu kimoja, kwani Waarabu wanakua wanafanya hivyo pale wanapokua wanaelezea vitu viwili ambavyo hua vinaendana pamoja, kama vile wanapoelezea kuhusiana Watu wawili ambao ni marafiki wasiotengana, au ndugu n.k hua wanatumia jina la mmoja aliekua maarufu miongoni mwao.**

Na andio maana Wanazuoni wakawa wana usemi usemao : 'Kutokana na Hadith za Al Umaran Umar wawili, au kauli za Umar wawili' wakimaanisha Umar Ibn Al Khattab *Radi Allahu Anhu*na Abu Bakar Al Siddiq *Radhi Allahu Anhu* kama wanavyosema *Al Qamarayn* Kumaanisha Jua na Mwezi'*(Lisan Al Arab).*'

Hivyo inaposemwa kua: **'Hii ni Sunna ya Umarayn basi hua kamwe haimaanishi Umar Ibn Al Khattab na Umar IBn Abd Al Aziz *Radhi Allahu Anhum,* kwa sababu ya kua maneno haya *Umarayn* asiliyake ni katika wakati wa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* kuwaelezea *Amir ul Muuminin* wawili wa mwanzo ambao ni Abu Bakar *Radhi Allah Anhu* na Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allah Anhu* kabla ya kujaUmarIbn Abd Al Azizi *Radhi Allahu Anhu.*'**

Na hii pia ni kutokana na kua Waarabu hua ni wenye kupenda kutumia Urahisi katika Lugha kimatamshi kwa maana hio tunapozungumzia kuhusiana na *Amir ul Muuminin* wawili wa mwanzo ambao ni Abu Bakar *Radhi Allah Anhu* na Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allah Anhu* kuitwa Umarayn basi hii haimaanishi kua Usemi huuu kua ni wenye kumpandisha juu kidarja Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allah Anhu*kuliko Abu Bakar *Radhi Allah Anhu* balini kutokana na urahisi wa matamshi yaani kutamka*Umarayn*huya kuna wepesi zaidi kuliko kutamka *Abu Bakaratayn.*

Ambapo mfano mwengine pia tunauona katika Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: **'Baina ya Kila *Adhanatayn* (Adhana Mbili) hua kuna Sala kwa kila atakaetaka Kusali baina yake' wakati Kinachozungumziwa hapa sio baina ya Adhana mbili za Salat Al Fajr au za Sala ya Ijumaa, bali ni baina ya Adhana na Iqamah za Sala moja.'**

Na pia kama ilivyotumika katika hadith isemayo: **'Baina ya Wafanyabiashara wawili hua kuna hiari pale itakapokua bado hawajaachana' wakati Hadith hii ni yenye kuwazungumzia Muuzaji na Mnunuzi.**

Na katika Al Taraz Al Awal imetajwa kua: **'Al Aswadayn hua iamaanisha Maji na Tende, Nyoka na Nge, Usiku na Joto na Macho Mawili.'***(Taraza Al Awwal)*

Na pia imesemwa kua : '**Ni Tende na Maji, ambapo Tende ni kutokana na weusi wake kama zilivyo Tende za Mji wa Madina hivyo Maji yameongezewa juu yake kutokana na ni kua yenye kuiga Rangi ya kitu yanapokua pamoja nacho, na Waarabu hua wanatumia Lugha hii ya kufananisha viti viwili kwa kimoja kilichomaarufu miongoni mwao kama vile Qamarayn au Hayatayn'***(Al Nihaya Fi Gharib Al hadith)*

Na pia Aswadayn imeelezewa kua: '**Ni Tende na Maji ambayo yote hua yanaelezewa kua ni vitu Vyeusi kama wanavyosema Waarabu kua: 'Kama Weusi ukitokea basi Weupe hua ni wenye kupungua, na Weupe Ukitokea basi Weusi hua ni wenye kupungua, kumaanisha Weusi kua ni Tende na Weupe kua ni Maziwa ''***(Al Faiq)*

Hivyo mbali ya kua Imeruhusika Kuua Wadudu ndani ya Sala, lakini pia kufanya hivyo Hua ni Sunna kutokana na Ukubwa wa Madhara unaoweza kusababishwa na Wadudu hawa kutokana na Ukali wa Sumu zao pale watakapomtafuna Mtu.

Ambapo anasema Al Hafidh Al Kabir Al Muharriri Imam Zayn Ad Din Abd Rahman Al Iraqi Al Shafii kua: '**Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na Miongoni mwa Watu Wenye Ilm walikua wakiifanyia kazi Hadith hii, na hii imesema pia na Imam Ahmad na Imam Is-haq Ibn Rahawayh**. **Wakiwemo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Umar *Radhi Allahu Anhu* n.k.**

Ambapo Imam Ibn Abi Shaybah amenukuu **Hadith ya Ali Ibn Abi Talib*Radhi Allahu Anhu* ambae alikua anasali na akaona Unyoya, ambao alifikiria kua ni Nge, na hivyo Akapiga na Kiatu chake.**

Ambapo Imam Al Bayhaqi amesema katika Hadith hii pia na kusema kua:**'Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* alilipiga Teke Nyoya hilo, na kisha kusema kua: Nilidhania kua ni Nge.'***(Sunnan Al Kubra)*

Miongoni mwa wenye Kuifanyia Kazi Hadith hii pia ni Imam Hasan Al Basr, Imam Abu Aaliyah Al Mawsil, Imam Ataa, Imam Muwarriq Al Ajli na wengineo. Na Amesema Mujtahid Imam Abu Bakr Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua: **'Kumuua Nyoka au Nge katika Sala hua kunaruhusika kwani hivyo ndivyo wasemavyo Wanazuoni. Ibn Umar aliona Unyoya na akafikiria kua ni Nge hivyo akaupiga kwa kiatu chake' na miongni mwa wanaosema kua inaruhusika kumuua Nge ndani ya Sala nipamoja na Al Hasan Al Basr, na wanaosema kua inaruhusika kumuua Nyoka au Nge ndani ya Sala ni Al Shafii, Ahmad Ibn Hanbal, Is-haq Ibn Rahawayh, Nuuman Ibn Thabit Abu Hanifa na wenzake.**'*(Al Awsat)*

Kwani anasema Na Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Farra Al Baghawi Al Shafi kua: **'Abu Sulayman amaesema kua: Hii inamaanisha kua kitendo ambacho ni kidogo kiuchache ndio kinaruhusiwa ndani ya Sala, na hivyo kukifanya mara moja au mara mbili hua hakubatilishia Sala, kwa sababu Kumuua Nge hua inawezekana kwa kipigo kimoja au viwili, lakini kama ikiwa kitendo hich kitarudiwa mara kadhaa na kuhesabika kua ni kingi basi Sala hubatilika**'*(Sharh Sunnah)*

Mbali ya kua Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi kua na Mtizamo usemao kua: '**Kama Mdudu husika hatokusumbua wala kukutia Khofu basi achana nae, usimfanye kit**u.'*(Musanaf Ibn Abi Shaybah)*

Ambapo Mtizamo huu ni wenye kufanana na Mtizamo wa Imam Ibrahim An Nakhai nae amesema pia kua: **'Hakika Kufanya hivyo hua ni Kujiondolea Khushuu ndani ya Sala.'***(Musanaf Ibn Abi Shaibah)*

Kwani anasema Shaykh Al Islami, Imam Al Muhaqqiqin, Al Allamaa Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Haythami Al Makki Al Shafii kua:

وَمَن تَلَبَّسَ بِصَومٍ تَطَوُّعٍ أو صَلَاةٍ أَو غَيْرِهِمَا مِن التَطَوُّعَات إِلّا النُّسُك، فَلَهُ قَطْعُهُمَا، لِلخَبَرِ الصَّحِيح: الصَّائِمُ الْمُتَطَوّعُ أَمِيرُ نَفْسِهِ إِنْ شَاءَ صَامَ وَإِنْ شَاءَ أَفْطَرَ'' وَقِيسَ بِهِ الصَّلَاة وَغَيرِهَا،فقوله تعالى:{وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ} مَحَلُّهُ فِي الفَرْضِ

‘Yeyote yule atakaefanya Ibada ya Sunnah kama Kufunga Au Kusali au Ibada nyengineyo, basi anayohaki ya Kuikatisha Ibada hio.Kama ilivyosemwa katika Hadith Sahih isemayo kua:

قال رَسولُ الله صلى الله عليه وسلم

"الصَّائمُ المتَطوّعُ أمِينُ نَفْسهِ، إنْ شاءَ صَامَ، وَإنْ شَاءَ أفْطَرَ":صَائمةً

Funga Ya Sunna ya Mtu hua ni yenye Kumilikiwa Na Mtu Husika, hivyo Mtu huyo kama akitaka Atafunga na akitaka Ataikatisha Funga hio.*(Sunnan At Tirmidhi)*

Na hii pia hua ni Kulingana na Sala na Ibada nyenginezo za Sunnah. Hivyo Maneno ya Allah *Subhanah wa Ta'ala* yasemayo:

:{وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ}

'Msizibatilishe Aamali Zenu" hua ni yenye Kuhusiana na Ibada za Fardhi.’*(Tuhfah Al Muhtaj Fi Sharh Al Minhaj)*

Na imesemwa kwenye Mawsuah Al Fiqhiyyah kua:

قَطْعُ العِبَادَةِ الوَاجِبَةِ بَعْد الشُّرُوعِ فِيهَا بِلَا مَسُوغٌ شَرْعِي غَيْر جَائِز بِاتِّفَاقِ الفُقَهَاءِ؛ لِأَن قَطَعَهَا بِلَا مَسُوغٍ شَرْعِي عَبَثٌ يَتَنَافى مَعَ حُرْمَةِ العِبَادَةِ

‘**Wanazuoni wanakubaliana kua kuibatilisha Ibada ya Fardhi bila sababu inayoruhusika baada ya kua imeshaanza hua hairuhusiki.Kwa sababu Kuibatilisha Ibada bila ya Sababu inayokubalika Kisharia hua ni kitendo kisichokua na maana ambacho hushusha thamani Utukufu wa Ibada husika.**’

Ila kama itakua kuna sababu inayokubalika Kisharia, basi hua inaruhusika, kwa mfano, kuibatilisha Sala kwa ajili ya Kumuua Nyoka au kwa ajili ya kuwaonesha watu wengine Nyoka ili wao wamuue.

أَمَّا قَطَعَهَا بِمَسُوغٍ شَرْعِي فَمَشْرُوعٌ، فَتَقْطَعُ الصَّلَاةَ لِقَتْلِ حَيَّةٍ وَنَحْوِهَا لِلأَمْرِ بِقَتْلِهَا، وَخَوْف ضَيَاع مَال لَهُ قِيمَةٌ، لَهُ أَو لِغَيْرِهِ، وَلِإِغَاثَةِ مَلْهُوف، وَتَنْبِيه غَافِل أَو نَائِمٍ قَصَدَتْ إِلَيهِ حَية ولَا يُمْكِن تَنْبِيهُهُ بِتَسْبِيح

Au Kwa mfamo kutoka na na Khofu ya Kupoteza Mali zako au za Waislam wengineo, Au kwa ajili ya Kumuokoa Mtu mwengine anaeomba Msaada wakoAu Kumuonya Mtu au kumuamsha

Mtu alielala pale anapokua anakaribiwa na Nyoka au Mnyama mwenye Madhara, Au Kumgutua Mtu asiekua na Habari juu ya Hatari inayomkaribia, pale inapokua haiwzekani Kumuonya au kumuokoa Mtu Husika kutokana na Tasbih yaani kusema Subhanah Allah.'*(Mawsuah Al Fiqhiyyah Al Kuwaitiyah)*

Na pia imesemwa kwenye Kashaf Al Qina kua:

وَيَجِبُ رَدُّ كَافِرٍ مَعْصُومٍ بِذِمَّةٍ أَو هدنَةٍ أَو أَمَانٍ عَن بِئْر، وَنَحْوِه، كَحَيَّةٍ تَقْصُدُهُ كَرَدِّ مُسْلِمٍ عَنْ ذَلِكَ بِجَامِعِ العِصْمَةِ، وَيَجِبُ إِنْقَاذُ غَرِيق وَنحوه كَحَرِيق، فَيَقْطَع الصَلَاةَ لِذَلِكَ فَرْضًا كَانَتْ الصَّلَاةُ، أَو نَفْلًا. وَظَاهِرُهُ: وَلَو ضَاقَ وَقْتُهَا، لِأَنَّه يُمْكِن تَدَارُكُهَا بِالقَضَاء، بِخِلَاف الغَرِيق وَنَحْوه ؛ (فَإِن أَبَى قَطْعُهَا) ، أَي الصَّلَاة لِإِنْقَاذ الغَرِيق وَنَحْوِه : أَثِمَ. انتهى

'Inaruhusika na hua ni Wajib kumuokoa hata Asiekua Muislam ambae Damu yake ni yenye kuheshimika kutokana na kua na Makubaliano nao ya Kusaidiana na Kiuslama, Kumuokoa kutokana na Vyenye Madhara kama Nyoka aliekua Karibu yake kama vile ambavyo inavyokua ni Wajibu kwa ajili ya Muislam mwenzakoKutokana na Utukufu wa Damu yake.

Hua ni Wajibu pia kumuokoa Mtu kutokana na Hatari kama Moto au Kuzama, hivyo katika hali kama hizi basi Mtu hua anatakiwa Kukatisha Sala yake.

Iwe Sala hio ni ya Sunnah Au ya Fardhi, Iwe Sala hio ndio kwanza imeanza au ndio inataka kumalizika, iwe mwanzo wa Wakati wa Kipindi cha Sala husika au Mwishoni mwa wakati wa Sala husika Kwa sababu Sala hio inaweza kulipwa hapo baadae kwa Kusaliwa Qadha.

Na kama Mtu akiwa anaendelea na Sala yake wakati kuna Mtu anazama na yeye hakumsaidia basi Mtu huyo anaesali hua ni mwenye kuhesabika kua ni mwenye kufanya dhambi mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.'**(Kashshaf Al Qina)*

Kwani anasema Sultan Ul Ulamaa, Mujtahid Shaykh Al Islami,Al Hafidh Imam Abu Muhammad Izz Ad Din Abd Al Aziz Ibn Abd Salam Ibn Abi Al Qasim Ibn Hasan Al Sulami Al Shafii kua:

تَقْدِيمُ إِنْقَاذ الغَرْقَى المِعْصُومِين عَلَى أَدَاءِ الصَّلَاة لِأَنَّ إِنْقَاذُ الغَرْقَى المِعْصُومِينَ عِندَ اللهِ أَفْضَل مِن أَدَاءِ الصَّلَاة، وَالجَمع بَينَ المِصْلَحَتَين مُمْكِنٌ بِأَن يُنقِذَ الغَرِيق ثُمَّ يَقْضِي الصَّلَاة. وَمَعْلُومٌ أَنَّ مَا فَاتَهُ مِن مَصْلَحَةِ أَدَاءِ الصَّلَاة لَا يُقَارِبُ إِنْقَاذُ نَفْس مُسْلِمَة مِنَ الهَلَاك

Kumuokoa Mtu Anaezama hua Kunatakiwa Kupewe Kipaumbele zaidi Kuliko Sala. **Na hii ni kwa sababu Kumuokoa Mti anaezama kumepewa Kipaumbele na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuliko Kusali**. **Na vyote hivi pia hua vinaweza kutekelezwa kwa mpangilio sa Kumuokoa anaezama kwanza na kisha Kulipa Sala**. **Kwani Kama tunavyojua kua kama Mtu akikosa Maslahi ya kuisali Sala ndani ya Wakati wake hua si sawa na kukosa Maslahi Makubwa zaidi ya Kuokoa Uhai wa Mtu au Kumuokoa kutokana na Madhar**a.'*(Qawaid fi Al Ahqami fi Al Islah Al Anam)*

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu baada ya **Bismi Allahi Al Rahmani Al Rahim** kua:

﴿بِسْمِ اللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۞ قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ۞ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَوٰتِهِمْ خَٰشِعُونَ﴾

Qad aflaha almu/minoona; Alladheena hum fee salatihim khashiAAoona. *(Surat Al Muuminun 23:1-2)*

Tafsir; ***Kwa Hakika Wamefuzu Waumini; Wale Ambao Ndani ya Sala zao wana Unyenyekevu.***

Ambapo hizi ni Aya ambazo tumeshazitafsiri mara kadhaa katika Kuelimishana kwetu. Na ndani yake tunaona kua zinatuhimiza umuhimu wa Kua na Khushuu katika wakati wa Ibada ya Sala kwani Kua na Khushu ndio kunakoipelekea Sala ya Mtu husika Kupanda Darja ya Juu na Kumpelekea Mtu husika kua ni mwenye Kufuzu.

Kwani Khushuu hua ni hali ya Utulivu wa hali ya juu unaotokana na Kuuhudhurisha Moyo ndani ya Ibada ya Sala. Na kuondoa Kila Kitu ndani ya Moyo wako Isipokua Uwepo wa Mola wako Ndani ya Moyo wako na Mbele yako. Ambako hua Kunakotokana na Mtu kujihisi kua yuko mbele ya Mola wake, yaani kama ilivyosema Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Jihisi kua Uko mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na anakuona hata kama wewe humuoni.

Hivyo bila ya shaka, kutokana na Maumbile ya Ibn Adam basi Khushuu hua haiwezekani kupatikana pale inapokua kuna Dharura itakayopelekea kukosekana Utulivu ndani ya Ibada ya Sala. Hivyo dharurah inayokubalika kukatisha Sala hua ni ile ambayo itapelekea kutokea Maangamizo ya Nafsi, Mali au Kitu. Hivyo Dharurah inayoruhusika haiwi ni ya Kuzama kwa Mtu tu, au Kutokea kwa Wadudu au Wanyama wanaodhuru tu, Au Moto.

Lakini pia ndani yake huingia mfano wa Mtu anaepika Nyumbani kwake na kisha akawacha chungu jikoni,na kuenda kusali na kisha chakula kikaanza kuungua. Ambapo katika Hali kama hii hua pia inaruhusika kukatisha Sala kwa sababu huenda kama Ukiiwacha Sufuria Au Kikaango kwenye Moto hadi Kikaungua basi itatokea Mripuko wa Moto utakaosababisha Madhara makubwa sana, aidha ya kuungua kwa nyumba na mali zako na huenda na wewe mwenyewe pia ukaungua kutokana nao Moto huo.

Mfano mwengine pia ni wa Mama mwenye Mtoto mdogo tuseme kama anaetambaa ambae atakua amemuacha Kitandani labda, na akaingia katika Sala, kisha akasikia Mtoto analia kwa Kilio cha Kushtusha basi bila ya shaka hii hua pia ni dharurah inayokubalika kukatisha Sala ili kuangalia Kimetokea nini, n.k.

Na bila ya Shaka, ukishaikata Sala basi hutakiwi kuirudia ulipoikatia, bali unatakiwa uanze upya tangu mwanzoni.

Hivyo kutokana na Hadith ya kuruhusika kuua Al Aswadayni ndani ya Sala basi Wanazuoni wanasema kua:**'Kutajwa Nyoka na Nge hua kunamaanisha kua inaruhusika Kuua pia Wanyama na Wadudu wote wenye Kusababisha Madhara, wakiwemo hata Nyigu, Mijusi n.k.**

Ambapo Miongoni mwa mifano pia ya Dharura zinazopelekea kuruhusika Kukatisha Sala ni pamoja na:

Inaruhusika Kukatosha Sala pale Mtu anapoanguka Ghafla, na hivyoKutakiwa kupatiwa msaada iwe mtu huyo yumo ndani ya Sala pamoja nawe katika safu Moja au nje ya Sala.

Inaruhusika Kukatisha Sala pale inapokuaKaribu ya Eneo Husika Kuna Shimo La Kisma au la Kitu chengine na Kisha ikawa Anakuja Mtu àmbae ni kipofu, na hivyo haoni na hajui na hivyo huenda akatumbukia ndani ya Shimo hilo na Kudhurika, au anapotokea hata Mtoto Mdogo pia anaekhofia kua anaweza kuingia kwa kutojua n.k.

Inaruhusika pia kukatisha Sala kutokana na Khofu ya Moto, Mnyama Mkali au Adui yako anaetaka kukudhuru.

Na amesema Al Hafidh, Al Faqih Imam Abd Rahman Ibn Ahmad Ibn Rajab Al Hanbal kua:**'Amesema Imam Qatadah Al Sadusi kua, Kama Mtu akiwa anasali na Kisha akaibiwa Mkoba wa Nguo zake, basi Mtu huyo anaruhusika kukatisha Sala na Kumkuzia Mwizi.'**

'Na anasema Imam Abd Razzaq kua: 'Amesema Muammar kua amesema Al Hasan na Qatadah kua Kama Mtu akiwa anasali na kisha akakhofia kua Kipando chake kitatoweka, au kitavamiwa basi anaruhusika kukatisha Sala'

Na amesemaAl Muafi kua Amesema Imam Sufyan Ath Thawry kua: 'Kama kikitokea Kitu cha Dharura kwa Mtu anaesali basi Mtu huyo anaruhusika Kukatisha Sala, na pia Kama akikhofia Mafuriko au Kipando chake.'

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: 'Kama Mtu alikua akimfuata Mdaiwa wake na kisha Mdaiwa huyo akaingia kwenye Sala na yeye pia akaingia kwenye Sala, na kisha Mdaiwa akakimbia kutoka kwenye Sala basi na anaemdai pia anaruhusika Kukatisha na kumfukizia.' *(Fat-h Al Barr Imam Ibn Rajab Al Hanbali)*

Ambapo hio ni kuhusiana na Sala ya Fardhi lakini kwa upande wa Sala ya Sunnah basi Wanazuoni wametofautiana juu ya kuruhusika kuikatisha baada ya Kuingia ndani yake.

Kwani kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kuaHaikubaliki Kuikatisha Ibada ya Sunna baada ya Kuingia Ndani yake isipokua kwa Kisingizio Kinachokubalika KishariaKama vile ilivyokua kwa upande wa Ibada ya Fardhi, hivyo hua ni lazima imalizwe kwa Sababu Ibada hio hua ni kitendo cha KuabuduHivyo hua ni Wajibu kuianza na kuimaliza, n hairuhusiki kuikatisha.'*(Al Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaitiyyah)*

'Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: Inaruhusika Kukatisha Vitendo vyote vya Sunnah na isipokua Umra na Hajj, na hii ni kutokana na Hadith isemayo kua: Anaefanya Vitenso vya Sunna hua yeye mwenyewe ndio Msimamizi wake vitendo hivyo' Lakini hata hivyo hua inapendekezwa Kuvimaliza vitendo hivyo

Ama kuhusiana na Hajj na Umra basi ni Lazima kumalizia kwa sababu Vitendo vya Sunnah vya Umra na Hajj hua ni Sawa na Vitendo vyake vya Fardhi.'*(Al Mawsuat Fiqhiyyah Kuwaitiyyah)*

Ambapo amesema Shaykh Ul Islami Imam Ahu Zakariyah Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: **'Atakaefanya Kitendo cha Sunna iwe Funga au Sala basi anaweza kuikatisha bila ya kua na Wajibu wa Kuilipa.'***(Al Minhaj)*

Na akasema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Vitendo vyote vya Sunna Hukmu yake hua ni sawa na Hukmu ya Funga ya Sunna yaani vinaweza kukatishwa bila ya kulipwa baada yake isipokua katika Hajj na Umra.'***(Al Mughni)*

Na amesema Imam Ahmad Ibn Muhammad At Tahtawi Al Hanafi kua: '**Kukatisha Sala hua hairuhusiki isipokua kwa Dharurah Maalum, ambapo kuna Baadhi ya Dharurah hua ni Wajib kukatisha Sala juu yake. Na mtu akikatisha Sala basi hua ni Wajib kuirudia upya Sala hio, iwe Sala ya Fardhi au ya Sunna.'***(Hashiya Al Tahtawi ala Maraqi Al Falah)*

Tumalizie kuhusiana na Mjusi alieruhusiwa na pia kupendekezwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuuliwa na ile Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا أَبُو كُرَيْبٍ، حَدَّثَنَا وَكِيعٌ، عَنْ سُفْيَانَ، عَنْ سُهَيْلِ بْنِ أَبِي صَالِحٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " مَنْ قَتَلَ وَزَغَةً بِالضَّرْبَةِ الأُولَى كَانَ لَهُ كَذَا وَكَذَا حَسَنَةً فَإِنْ قَتَلَهَا فِي الضَّرْبَةِ الثَّانِيَةِ كَانَ لَهُ كَذَا وَكَذَا حَسَنَةً فَإِنْ قَتَلَهَا فِي الضَّرْبَةِ الثَّالِثَةِ كَانَ لَهُ كَذَا وَكَذَا حَسَنَةً

Amesema Abu Kurayb kua amesema Wakii kua amesema Sufyan kua amesema Suhayl Ibn Abi Salih kua amesema Baba yake kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaeua Wazagh (Aina ya Mjusi) kwa pigo la kwanza basi atakua na Malipo Kadhaa ya Thawabu. Atakaemuua kwa mapigo mawili atapata thawabu ambazo ni kidogo zaidi ya alieua kwa pigo moja. Na atakaemuua kwa mapigo matatu atapata Malipo ya Thawabu ambazo ni chini kidogo ya alieua kwa mapigo mawili.'*(Sahih Bukharin a Muslim, Sunnah Tirmidhii)*

Naam..inabidi tuiangailie hadithi hii kwa sababu ya Ujumbe uliomo ndani yake ambao ni wenye Kuamrisha Kuuliwa kwa Mdudu aina ya Mjusi mwenye Madhara ambae katika Hadith hii ametajwa kwa jina la Wazagh.

Na kama tulivyofahamishana hapo awali kua Inaruhusika kukatiaha Sala kaa ajili ya Kuua Mdudu au Mnyama anaeweza kusabisha Madharakama Nyoka na Nge, hivyo baadhi wanaweza wakajiuliza kuhusiana na huyu Wazagh ambae pia ameamrishwa kuuliwa ni Mjusi wa aina gani? Au Mijusi wa aina zote?

Hivyo ingawa Takriban kila Mtu ameiyafsiri hadith hii kua ni yenye kumaanisha Mijusi wa aina zote, lakini hata hivyo tunapoangalia kwa upande wa Wanazuoni basi waoWanasema kua:

Si Kila aina Ya Mjusi hua ni Wazagh, kwani Wazagh hua ni Mjusi mwenye Sifa zifuatazo:

1-Ni Mdudu Anetambaa na anaesababisha Madhara.

2-Ni Mdudu ambae ana Miguu ambae hua anatembea kwa kasi katika Vishina vya Majani.

3-Ni Mdudu ambae hua anakunywa Maziwa Ya Ngamia kwa Kunyonya Chuchu za Ngamia.

4-Ni Mdudu ambae anaishi Kwenye Dari na Kuta za Nyumba na hua ni mwenye Kulia kwa kutoa sauti kali.

Na hii ni kama ilivyoelezewa na Imam An Nawawi katika *Sharh Sahih Muslim,* Imam Badr Ad Din Al Ayni katika Umdat Al Qari Sharh Sahih Bukhari,Imam Muhammad Shams Al Abadi katika *Awnul Maabud,* Imam Muhammad Tahir katika *Majmaa Bihar Al Anwar Sharh As Sahihayn.*

Na amesema Imam Shuhab Ad Din Abu Abd Allah Fadhil Allah Ibn Hasan Ibn Husayn Ibn Yusuf Ibn Al Turishti Al Hanafi kua: '**Wazagh hua ni Mdudu Mdogo ambae kutokana na Jina lake hua ni mwenye kasi kubwa sana katika kutambaa kwake.'***(Muyassar fi Sharh Masabih Sunnah)*

Hivyo Wanazuoni wanasema kua Wazagh hua Si Mjusi Mkubwa Sana na wala Si Mdogo sana.

Ambapo amesema Al Muhaqiq Kalamu Ad Din Imam Ad Dumayri Al Shafii kua: '**Wanazuoni wetu wanasema kuhusiana na Wanyama na Wadudu wote ambao hawasababishi Madhara. Na Wala Hawana Manufaa kama Nyungunyungu,Ndege wadogo, Ndege wakubwa wanaokula Nyama,Mijusi wenye Miba mgongoji, n.k hua ni Makruh kuwaua iwe kwa Mtu aliekua katika Ihram ya Ibada ya Hija au Nje yake.**

Na amesema Imam Ibn Abd Al Barr kua: **'Kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua Inaruhusika Kuu Panya, Buku, Nge, Nyoka, na Wazagh nje na ndani ya Masjid Al Haram.'**

Al Muhaqqiq Kalamu Ad Din Imam Ad Dumayri Al Shafi anasema tena kua: '**Ama kuhusiana na Wazagh basi hua ni Fuwaysiq(Mdudu Mbaya sana) ambae yumo katika Al Fawasiq Khams(Wadudu Watano walioruhusika Kuuliwa ndani na nje ya Masjid Al Haram)**

Ambapo neno Fuwaysik limetokana na neno Fisq ambalo ni lenye kumaanisha Kua na utofauti na Wanyama wengineo wote kwa Ukubwa wa Madhara yao.

Ambapo Imam Bukhari amenukuu kutoka kwa Ummi Sharik *Radhi Allahu Anha,* Kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha Kuuliwa kwa Wazagh na kusema kua: Alikua ni mwenye Kupuliza Moto aliowashiwa Nabii Ibrahim.'*(Hayat Al Hayawan Al Kubra)*

Ambapo amesema Imam Mula Al Qari Al Hanafi kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha kuuliwa kwa Mjusi wa aina ya Wazagh ambae ni Mdudu Mwenye Madhara Makubwa.'**

Na akasema Imam Al Shirwani Al Shafii kua: '**Kutokana na kua Wazagh wa wakati wa Nabii Ibram ndie aliepulizia Moto alioingizwa Nabii Ibrahim basi hili limekua ndio thibitisho la Ubaya wa Madhara ya Wazagh na pia ni sehemu ya Kumheshimisha Nabii Ibrahim.'***(Hashiyat Tuhfa Al Muhtaj)*

Na akasema Imam Ibn Malak kua: '**Wazagh hua anapenda Kuharibu Chakula hususan Chumvi, kiasi ya kua kama hakupata njia ya Kuiharibu basi atapanda juu ukutani na kisha kuitia Kinyesi chake, hivyo Hadith hii inaainisha Madhara yake***.'(Mirqat Al Mafatih)*

Na akasema Imam Ibn Al Arabi Al Maliki kua: **'Wanyama na Wadudu wamegawika Katika Makundi Mawili ambayo ni wenye Kudhuru na wasodhuru.**

Hivyo Wale wanaaosababisha Madhara basi hua inaruhusika kuwaua na wasiosababisha Madhara hua hairuhusiki kuwaua. Na Wazagh ni Mdudu ambae ni mwenye Madhara, kwani ni mwenye Kuharibu chakula na kuweza kumsababishia kifo anaekula chakula hicho alichokiharibu. Hivyo ni Wajibu Kumuua na pia kuwaua Wadudu kama hawa.'

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi akasema kua: **'Wanazuoni wanakubaliana kua Wazagh hua anaingia katika Wadudu wenye Sumu na *Rasul Allah Salallahu Alayh wa Salam* ameamrisha na Kuwatia Ari watu kua wamuue kwa sababu ya Madhara yake.'***(Sharh Sahih Muslim)*

MUBTILATAL SALAT - YANAYOBATILISHA SALA

❖❖❖❖

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na mambo yanayobatilisha Sala, basi tunaona kua yako mengi ingawa Wanazuoni wametofautiana juu ya baadhi ya Mambo hayo.Hivyo nasi tutajaribu kuangalia kwa kadri tutakavyoweza kulingana na hali na Mazingira ya Waliotangulia kabla yetu na sisi pia.

Na ninasema hivi kwa sababu ambazo tutaziona hapo baadae Inshaa Allah katika Kufafanua kwetu.Ila yanayojulikana wazi kua yanabatilisha Sala kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni ni Yafuatayo:

1-Kubatilika kwa Udhu.
2-Kuonekana kwa sehemu za Siri ambazo hazitakiwi kuonekana mbele za Watu.
3-Kutoelekea Kibla.
4-Kua na Najis aidha kwenye Nguo ya Mtu anaesali, au kwenye Sehemu anayosalia.
5-Kukosa Utulivu Ndani ya Sala kwa kufanya Vitendo visivyostahiki kwa idadi ya wingi.
6-Kuvunja Nguzo ya Sala kwa Makusudi.
7-Kuongeza Nguzo ya Sala kwa makusudi.
8-Kupangua Mpangilio wa Nguzo za Sala kwa Makusudi.
9-Kutoka Ndani ya Sala kabla ya Mda kwa kutoa Salam kabla ya kumaliza Sala.
10-Kubadilisha Maana ya Aya au Visomo vya ndani ya Sala.
11-Kuvunja Nia ya Sala kwa Makusudi kutokana na Kuamua kutoendelea Kusali.
12-Kucheka kwa Sauti.
13-Kuzungumza Ndani ya Sala Maneno yasiyohusiana na Sala.
14-Kuzimia,kuingia Wazimu au Kufariki ndani ya Sala.
15-Kutekeleza Nguzo ya Sala kabla ya Imamu.
16-Maamuma kuzikosa Hatua Mbili za Imam wake ambazo ni miongoni mwa Nguzo husika.
17-Kusali baada ya Kutayamam na kisha Kuona Maji wakati uko ndani ya Sala.
18-Mtu Anaesali Kumkosoa Mwengine ambae Ni mwenye Kusali Sala tofauti nae

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- HADATH

❖❖❖❖

Neno Udhu linatokana na neno Udhu ambalo hua ni lenye kumaanisha Usafi na Tohara, hivyo Udhu hua ni mpangilio maalum wa njia ya kujitoharisha kwa kukosha baadhi ya viungo vya mwili wa Ibn Adam kwa kutumia Maji. (*Mu'tamad Fi Al-Fiqh Al-Shafii*)

Na kama tulivyosema kua Sala hukamilika pale inapokua zimekamilika Nguzo za Sala, na Pia Yamekamilika Masharti ya Sala.Kwa maana hio basi inapokosekana moja kati ya Nguzo za Sala au Moja kati ya Masharti yake basi Ibada ya Sala pia hubatilika.

Ambapo tunapozungumzia kuahusiana na Kubatilika kwa Sala basi tunaona kua Wanazuoni wa Ilm ya Fiqh wamekua wakitumia maneno mawili kumaanisha Batiliko la Ibada ya Sala ambayo ni:

1-*Batil* linalotokana na neno *Batala* ambalo maana yake hua ni Batili, Bure, Haribika, Isiokua na Thamani, Isiokua na Maana, Iliyofutwa Malipo yake,Isiokua ya Haki, Isiokua ya Kweli na pia humaamisha Potovu.

2-*Fasid* linalotokana na neno *Fasada* lenye kumaanisha Kuharibika, Kufisidika, Kuoza, Kutokukubakika, Kua ni yenye Uasi, Kua mbaya, Kufanya Ubaya na pia humaanisha Kufanya Uhuni.

Kwa maana hio basi nadhani haitokua na haina haja kufafanua zaidi kuhusiana na maana ya Kubatilika kwa Udu au Kufisidika kwa Udhu ambako ndiko pia kunakopelekea Kubatilika au Kufisidika kwa Sala**.**

Hivyo kuna Makubaliano ya wanazuoni kuhusiana na Utumiwaji wa maneno mawili haya ya Batil na Fasid kuhusiana na Ibada ya zote za Kiislam.

Ambapo makubaliano hayo ni kwa upande wa Wanafiqh wa Madhhab ya Imam Malik, Imam Ak Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal tu.Kwani kwa upande wa Wanafiqh wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wametofautisha kuhusiana na Utumiaji wa maneno haya hususan katika Miamalati ya Makubaliano ya Ndoa, Mikataba, Mauziano n.k

Na ingawa kuna kukubaliana juu ya utumiwaji wa Maneno Mawili hayo basi sisi katik kufahamishana kwetu tutakua ni wenye kutumia zaid asili ya neno Batala lenye kumaanisha Kubatilika, ingawa pia huenda nikajisahau nikatumia neno Kufisidika, au kama nikitaka kutilia mkazo zaid basi huenda nikatumia neno Fisidika.

Naam..hivyo miongoni mwa Yanayobatilisha Sala hua ni Kubatilika kwa Udhu. Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Ufunguo wa Pepo ni Sala na Ufunguo wa Sala ni Udh**u.'*(Imam At Tirmidhii)*

Hivyo kabla hatujazungumzia kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu kwa kina basi kwanza na Tukumbushane kuhusiana na Udhu japo kwa kifupi.

Ambapo amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* baada ya *Bismi Allahi Rahmani Rahim* kua:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ إِذَا قُمْتُمْ إِلَى ٱلصَّلاةِ فٱغْسِلُواْ وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى ٱلْمَرَافِقِ وَٱمْسَحُواْ بِرُؤُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى ٱلْكَعْبَينِ وَإِن كُنتُمْ جُنُباً فَٱطَّهَّرُواْ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ ٱلْغَائِطِ أَوْ لاَمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيداً طَيِّباً فَٱمْسَحُواْ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِّنْهُ مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

Yaaa aiyuhal ladheena aamanoo izaa qumtum ilas Salaati faghsiloo wujoohakum wa Aidiyakum ilal maraafiqi wamsahoo biru'oosikum wa arjulakum ilal ka'bayn; wa in kuntum junuban fattahharoo; wain kuntum mardhaaa aw'alaa safarin aw jaaa'a ahadum minkum minal ghaaa'iti aw laamastumunnisaaa'a falam tajidoo maaa'an fatayammamoo sa'eedan taiyiban famsahoo

biwujoohikum wa aideekum minh; ma yureedul laahu liyaj'ala 'alaikum min harajinw walaakiny yureedu liyutahhirakum wa liyutimma ni'matahoo 'alaikum la'allakum tashkuroon. *(Surat An Maidah 5:6)*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Mtakapokusudia Kusimamisha Sala, basi kosheni nyuso zenu na mikono yenu hadi kwenye visugudi, futeni (kwa kutia maji mikono yetu) vichwa vyenu, na mkoshe miguu yenu hadi kwenye kifundo chake. Ikiwa mko katika hali ya Janaba, basi jitoharisheni. Lakini ikiwa mnaumwa au mko safarini au mkiwa mmetoka kujisaidia au lamastumu alnnisaa (mkiwa mmegusana na wanawake) na hamkupata maji yeyote, basi fanyeni Tayamam kwa kutumia mchanga ulio safi na mjipanguse kutokana nao katika mikono yenu na nyuso zenu. Allah hataki kukujaalieni ugumu katika mambo, bali anataka kukutoharisheni, na mkamilishealiyokufanyieni juu yenu ili muwe wenye kushukuru.***

Ambapo hii ni aya inayoainisha Viungo 7 vya Fardhi katika Kutia Udhu kama ilivyosemwa kwenye Sahih Bukhari kua:

وَقَوْلِ اللَّهِ تَعَالَى: {إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلاَةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ} قَالَ أَبُو عَبْدِ اللَّهِ وَبَيَّنَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّ فَرْضَ الْوُضُوءِ مَرَّةً مَرَّةً، وَتَوَضَّأَ أَيْضًا مَرَّتَيْنِ وَثَلاَثًا، وَلَمْ يَزِدْ عَلَى ثَلاَثٍ، وَكَرِهَ أَهْلُ الْعِلْمِ الإِسْرَافَ فِيهِ وَأَنْ يُجَاوِزُوا فِعْلَ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ.

Na kuhusiana na kauli ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* isemayo kua:*Enyi mlioamini! Mtakapokusudia Kusimamisha Sala, basi kosheni nyuso zenu na mikono yenu hadi kwenye visugudi, futeni (kwa kutia maji mikono yetu) vichwa vyenu, na mkoshe miguu yenu hadi kwenye kifundo chake, basi amesema Abu Abd Allah (Muhammad Idris Al Shafii)kua:*

***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameweka wazi kua ni Wajibu katika wakati wa Kutia Udhu Kuzikosha sehemu zilizotajwa kwenye Aya hii mara moja Na yeye *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua Akitawadha huzikosha Sehemu hizi mara mbili au tatu, lakini kamwe hakua akizikosha zaidi ya mara Tatu'** *(Al Umm – Sahih Bukhari)*

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akafafanua Viungo 8 vya Sunna za Udhu kwa kufundisha kwa vitendo kutia udhu kama ilivyosemwa tena kwenye Hadith zifuatazo kua:

حَدَّثَنَا أَبُو الْيَمَانِ، قَالَ أَخْبَرَنَا شُعَيْبٌ، عَنِ الزُّهْرِيِّ، قَالَ أَخْبَرَنِي عَطَاءُ بْنُ يَزِيدَ، عَنْ حُمْرَانَ، مَوْلَى عُثْمَانَ بْنِ عَفَّانَ أَنَّهُ رَأَى عُثْمَانَ دَعَا بِوَضُوءٍ، فَأَفْرَغَ عَلَى يَدَيْهِ مِنْ إِنَائِهِ، فَغَسَلَهُمَا ثَلاَثَ مَرَّاتٍ، ثُمَّ أَدْخَلَ يَمِينَهُ فِي الْوَضُوءِ، ثُمَّ تَمَضْمَضَ، وَاسْتَنْشَقَ، وَاسْتَنْثَرَ، ثُمَّ غَسَلَ وَجْهَهُ ثَلاَثًا وَيَدَيْهِ إِلَى الْمِرْفَقَيْنِ ثَلاَثًا، ثُمَّ مَسَحَ بِرَأْسِهِ، ثُمَّ غَسَلَ كُلَّ رِجْلٍ ثَلاَثًا، ثُمَّ قَالَ رَأَيْتُ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم يَتَوَضَّأُ نَحْوَ

وُضُوئِي هَذَا وَقَالَ " مَنْ تَوَضَّأَ نَحْوَ وُضُوئِي هَذَا ثُمَّ صَلَّى رَكْعَتَيْنِ، لاَ يُحَدِّثُ فِيهِمَا نَفْسَهُ، غَفَرَ اللَّهُ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ

Na amesema Abu Al Yaman kua amesema Shuayb kua amesema Al Zuhri kua amesema Ataa Ibn Yazid kua amesema Humran ambae ni Mtumwa alieachwa huru na Uthmani Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* kua:

Mimi nilimuona Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* akiomba Maji ya Kutawadhia Na alipoletewa akamimimina Maji hayo kutoka kwenye chombo chake juu ya mikono yake, na akakosha mikono kwa mkono wake wa kulia mara tatu.

Na kisha akatia Akasukutua na kutia Maji kwenye Pua yake, na kisha Akanawa Uso wake mara tatu tatu.

Kisha akakosha Mikono hadi kwenye Visugudi mara tatu.

Kisha akapangusa kichwa chake na akakosha Miguu yake kila mmoja mara tatu tatu. Kisha Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* akasema: Mimemuona Mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kama nilovyyotawadha mimi huu Udhu wangu.

Na kisha akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Mwenye Kutawadha Kikamilifu kama nilivyotawadha mimi na kisha akasali Rakaa mbili bila ya kufikiria chochote ndani yake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* humfutia Dhambi zake Mtu huyo zilizotangulia.'*(Sahih Muslim)***

Na katika hadith nyengine imesemwa kua: '***Amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua:***

من توضأَ كما أُمِرَ ، و صلَّى كما أُمِرَ ، غُفِرَ له ما قدَّم من عملٍ

'Yeyote atakaetia Udhu kama nilivyotia Mimi, na akasali kama nilivyosali mimi basi Dhambi zake ndogo zote zilizopita zitasamehewa'*(Sahih Muslim)*

Hivyo bila ya Shaka tunaopaingalia sehemu hii ndogo ya mwanzo wa Aya hii basi tunaona kua imeainisha sehemu 7 za fardhi za Udhu ambazo ni:

Nia.
Kukosha Uso Mzima.
Kukosha Mikono yote Miwili wa Kulia na Kushoto hadi kwenye Visugudi.
Kupaka Maji Juu ya Kichwa.
Kukosha Miguu yote Miwili hadi juu ya vifundo vya Miguu kwa kuanzia Mguu wa kulia kumalizia wa kushoto.
Kutia Udhu kwa mpangilio huu bila ya Kupititisha Mda mrefu baina yake.
Yaani Usikoshe Uso kisha ukasubiri hadi Maji yakakauka usoni kisha ndio ukakosha mikono n.k.

Na kulingana na Hadith basi tunaona kua Sunnah za Udhu ni 8 ambazo ni:
Kuanza kwa kukosha Viganja vyote viwili vya mikono.
Kusukutua.
Kupandisha Maji Puani na kuyatoa.

Kupaka Maji Kichwani kutokea Nyuma kuja mbele baada ya kumalizia kupaka kutoka mbele kuelekea Nyuma.
Kukosha Masikio yote mawili nje na ndani.
Kufuatilia Mpangilio huo.

Na bila ya shaka Udhu pia Mapendekezo yake ambayo ni:
Kuanza kwa kusema Bismi Allahi Rahmani Rahiim.
Kutia Udhu wakati ukiwa katika Sehemu ambayo ni Safi.
Kutofanya Israfu katika Utumiaji wa Maji katika Kutia Udhu.
Kuweka chombo chenye Maji ya kutilia Udhu katika upande wa Mkono wako wa kulia.
Kukosha Kila Kiungo kwa mara 3.
Kuanza kupakaza Maji Kichwani kutoka mbele ya Kichwa kuelekea Nyuma ya Kichwa.
Kupiga Msuwaki.
Kuanza kwa upande wa kulia katika kukosha Viungo vyote stahiki na kumalizia kwa upande wa kushoto.
Kufuatisha Mpangilio wa hatua za Utiaji Udhu

Na tunapoangalia kuhusiana na yanayokirihisha katika Kutia Udhu basi tunaona kua ni yafuatayo:

Kutia Udhu Katika Sehemu isiyokua Nadhifu.
Kufanya Israfu katika Utumiaji wa Maji katika wakati wa kutia Udhu.
Kukosha Viungo stahiki vya Udhu kwa zaidi ya mara 3.
Kupandisha Nguo Juu hadi ikawa hukustirika yaani ukaonesha sehemu za mwili wako zisizotakiwa kuonekana katika wakati wa kutia udhu hususan unapotia Udhu Mbele za Watu kama Msikitini.
Kukosha au kupaka Maji Shingo.
Kukosha sehemu ambazo hazikutajwa kua ni sehemu stahiki na hazimo kwenye Mpangilio wa Kutia Udhu.
Kupukutisha Maji yaliyopo kwenye viungo vya mwili wako yaliyobakia baada ya kutia Udhu.
Kuachana na Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Kutia Udhu, ambazo hua ni Sehemu za Sunna za Udhu.
Kuzungumza mazungumzo ya kawaida au maneno ya Kidunia au maneno ambayo hayahusiani na Udhu wako.

Mambo yasiyoruhusika kuyafanya bila ya kua na Udhu:

Kusali.
Kusujudu Sijdat Tilawah.
Kuzunguka Al Kaabah.
Kugusa Qur'an.

Inapendekezwa Kutia Udhu katika hali zifuatazo:

Unapotaka Kusimama kwenye Kisimamo cha Arafah na kufanya Sa'y au Kutembea kwa haraka harakabaina ya Safwa na Marwa.
Unapotaka kuadhini.
Unapotaka Kukosha na kubeba Mwili wa Maiti wa Kiislam.
Unapotaka Kusoma au Kusikiliza Qur'an.
Unapotaka Kusoma au Kuandika Vitabu vya Ilm ya Dini ya Kiislam.
Unapotaka kuingia Msikitini, Kukaa Msikitini Kutoa Khutba Msikitini.

Unapotaka kulala na mara baada ya Kuamka.
Utakapocheka kwa sauti wakati ukiwa ndani ya Sala.
Unapotaka Kungiliana Na Mwenza wako Kindoa, Unapotaka Kula.
Baada ya kua na Hasira au kufanya Dhambi kama ya Kusengenya n.k

MANUFAA YA UDHU KIMWILI NA KINAFSI

❖❖❖❖

Tunapoangalia manufaa ya Udhu Kimaumbile basi tunaona kua Udhu ni ngao dhidi ya vijidudu katika maisha yetu ya kila siku. Kutia udhu mara tano kwa siku kunaweza kukuepusha na magonjwa mengi. Uchunguzi wa kisasa umeonyesha kuwa Udhu ni kanuni ya dhahabu ya kulinda afya. Ambapo baadhi ya faida zake katika kila hatua zake ni:

Kukosha mikono: Katika kutia udhu, mtu anatakiwa kukosha mikono yote miwili hadi kwenye kifundo cha mkono mara tatu. Kwani baada ya hayo, mtu anapaswa kusuuza kinywa. Hivyo ikiwa mikono haijaoshwa, basi vijidudu vya mikono huingia mwilini kupitia mdomoni na kusababisha maradhi tofauti. Kwa kuwa watu hufanya vitendo vyao vyote kwa msaada wa mikono yao, ni kawaida kwa vijidudu kushikamana na Mikono. Ndio maana pia miongoni mwa Sunna za *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* ni kukosha mikono kabla ya Kula na Wanasayansi wamethibitisha hilo.

Kukosha Mdomo: Kukosha mdomo kwa kusukutua mara tatu hua ni Sunnah. kusukutua huondoa chembe za chakula zilizokwama kwenye meno, ambazo hukwama kati ya meno na kusababisha harufu mbaya ya kinywa. Wanasayansi wa matibabu wanasema kuwa meno kamili yanamaanisha afya njema. Hivyo kusukutua huweka meno safi na na yenye afya. Mbali na hili, kusukutua pia hua kunazuia magonjwa ya tonsil na koo.

Kukosha Pua: Pua ndiyo njia pekee ya kupumua. Na hewa ambayo inapumuliwa ina vijidudu vingi vyenye madhara, ambavyo huingia ndani ya mwili kupitia katka Tundu za Pua. Kwa hiyo, ikiwa unasafisha kwa Maji ndani ya Pua yako itatoka. Basi utakua ni mwenye kujizuia na kujiepusha na madhara haya Pia, ikiwa maji yataingia kwenye Pua na kuikosha, basi hata Ubongo hua ni wenye kuimarika, Macho huongezeka Nuru, na maradhi ya kuumwa na kichwa kutokana na madhara ya Pua na koo huoondoka.

Kukosha Uso: Kama tunajuua kua kuna vidudu vya Maradhi mengi yanayoelea angani, ambayo Jicho haliwezi kuona. Na kwa kuwa Uso wetu hua uko wazi kila wakati basi, vijidudu hivyo hujikusanya Usoni Mbali na hayo, chembe chembe za vumbi huruka na kuanguka usoni, matibabu pekee ambayo kwayo ni udhu. Wataalamu wa afya na urembo wanasema kuosha uso wako kila siku kunanufaisha urembo na afya njema. Mwanachama wa Baraza la Urembo la Marekani Lady Hitcher alisema Waislamu hawahitaji kutumia aina yoyote ya losheni ya kemikali. Kwani Hawezahujikinga na maradhi yote ya uso kwa Udhu. Kukosha Uso kunaweza kurudisha mng'aro wa ngozi ya Uso, wepesi na ulaini kwenye ngozi ya uso. Matokeo yake, Mwonekano unakuwa mzuri. Pia huimarisha ngozi ya macho na kuzuia magonjwa mbalimbali ya macho.

Kukosha mikono hadi viwiko vya mkono: Ni fardhi kukosha mikono yote miwili hadi kwenye visugudi. Inaongeza mzunguko wa damu kwenye mikono na kuimarisha misuli ya mikono. Mbali na hayo, mishipa ya mkono imeunganishwa na mishipa ya mwili mzima. Kwa hivyo ikiwa unakosha mikono yako hadi kwenye viwiko, athari huenea kwa mwili mzima. Kuosha mikono

hadi kwenye viwiko ni muhimu sana kwa Mfumo wamzunguko wa Damu wa Moyo na nguvu ya Nishati. Kwa sababu kuna aina tatu za mishipa mikubwa kwenye Visugudi, ambayo inahusiana na Moyo, Ubongo, na Ini. Kukosha mikono hadi kwenye visugudi hutia nguvu viungo vitatu hivyo na kuvilinda na magonjwa.

Kupangusa kichwa: Kichwa ndicho kiungo muhimu kuliko viungo vyote vya binadamu. Kusugua kichwa hupunguza kizunguzungu, baridi, na kukosa usingizi na kuboresha macho. Pia, Kuifuta kichwa kwa mikono ya iliyoroa maji huondoa vumbi lililokwama kwenye nywele. Utafiti wa kisasa umeonyesha kuwa masaji ya kichwa huponesha pia Maradhi ya sikio. Wakati wa kuifuta kichwa, tunaingiza vidole ndani ya sikio. Jambo ambalo linapelekea kusafisha Masikio na kuongeza uwezo wa kusikia. Kuifuta sehemu ya nje ya sikio kunaondoa ufupi wa kusikia.

Kuosha miguu: Miguu yetu ndiyo huathirika zaidi na vumbi na vijidudu. Kwa hiyo, Uislamu umetuamrisha kuosha miguu yetu mara tano kwa siku kwa njia ya udhu na kusafisha vidole vya miguu ili vijidudu vilivyoganda baina yake viweze kuondoka. Na pia huongeza mzunguko wa Damu. Moyo, Figo, Tumbo, na viungo vinahusiana na miguu. Kwa sababu hii, ikiwa unapokosha miguu yako, basi hua unapata unafuu wa maradhi kama ya kupoteza hamu ya kula, homa, kizunguzungu, udhaifu wa kijinsia, nk.

Kulingana na wanasayansi wa kitabibu, viungo vilivyooshwa kwenye Udhu vinanufaisha afya. Na imethibitishwa kua kumwaga maji kwa mikono miwili mwanzoni mwa Udhu huamsha mishipa ya mwili, kisha taratibu, athari zake hufika kwenye mishipa ya uso na ubongo. Kukosha mikono kwanza katika Wudhu, kisha Kukosha Mdomo, kisha kukosha pua, kisha kukosha Uso na sehemu nyingine—mpangilio huo ni wenye manufaa mengi sana kwa kuzuia Maradhi tofauti. Hospitali nyingi za kigeni zinakubali Udhu kama dawa ya kutibu wagonjwa wa magonjwa mbalimbali. Inaaminika kuwa kiwango cha matatizo ya msongo wa mawazo miongoni mwa Waislamu ni cha chini kutokana na matumizi ya Udhu mara 5.

Hivyo kwa kifupi basi Udhu Kiafya hunufaisha kwa mambo yafuatayo:
Kuboresha mfumo wako wa kinga ya Mwili.
Kuongeza kwingi wa Idadi seli nyekundu za damu kwa kuboresha harakati za Moyo.
Kuzuia vijidudu kuingia kwenye mwili.
Kulinda macho kutokana na mkusanyiko wa vumbi au jasho.
Kuimarisha Mfumo wa mzunguko wa damu.
Kuchochea Mapigo ya asili ya Kimaubile ya mwili.
Kuweka mwili wako harufu nzuri.

Ambapo kwa upande wa Kinafsi basi Manufaa yake hua ni mengi zaid na ni bora zaidi kwani amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Abu Daud kua:

فعن عبد الله بن بجير الصنعاني قال: دخلنا على عروة بن محمد السعدي، فكلَّمه رجل، فأَغضبه، فقام فتوضأ، فقال: حدَّثني أبي عن جدي عطية، قال: قال رسولُ الله صلى الله عليه وآله وسلم: «إِنَّ الْغَضَبَ مِنَ الشَّيْطَانِ، وَإِنَّ الشَّيْطَانَ خُلِقَ مِنَ النَّارِ، وَإِنَّمَا تُطْفَأُ النَّارُ بِالْمَاءِ، فَإِذَا غَضِبَ أَحَدُكُمْ فَلْيَتَوَضَّأ

Amesema Abdullah Ibn Bujayr Al-Sana'ani, Kua: 'Tuliingia kwa Urwah Ibn Muhammad al-Sa'di, na Mtu mmoja akamsemesha na kumkasirisha, hivyo Urwa nae akasimama na

**akatawadha, na akasema: Baba yangu aliniambia kwa mamlaka ya Babu yangu Atiyah, kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Hakika ya Ghadhabu hua ni zenye kutokana na Shaytani, na Shetani ameumbwa kutokana na Moto, na Moto huzimika kwa maji tu, basi kama mmoja wenu ataghadhibika, basi na atie Udhu.' *(Sunan Abu Daud, Musna Imam Ahmad Ibn Hanbal)*

Unapokua na Udhu basi Mtu hua na umakini zaidi juu ya Mola wako kutokana na kutokua na hamu ya kutotokwa na Udhuu wako na Hivyo unakua unamkumbuka Mala wako kila Wakati ambako nako huypelekea kupunguza Hasira kama anavyosema Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii kua: **'Fahamu kua kuna sababu za kutuliza hasira inapomshambulia Mtu ambazo zinaweza kutumika kumsaidia mtu kuwa na subira; Ikiwa ni pamoja na: kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta'ala* ; Hili humsukuma kumuogopa, na kumwogopa humsukuma kumtii, hivyo hurejea katika adabu zake na kufuata mawaidha yake. Kisha hasira huondoka: kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿وَٱذۡكُر رَّبَّكَ إِذَا نَسِيتَ﴾

Waudhkur Rrabbaka Iadha Nasiita*(Surat Al Kahf: 18:24)*

Tafasir: ***Na mkumbuke Mola wako Mlezi unaposahau.****(Adab Al-Dunya Wa Al-Din)*

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

إذا توضَّأَ العبدُ المسلمُ – أوِ المؤمنُ – فغسلَ وجهَهُ ، خَرجَت مِن وجهِهِ كلُّ خطيئةٍ نظرَ إليها بعَينيهِ معَ الماءِ – أو معَ آخرِ قطرِ الماءِ ، أو نحوَ هذا – فإذا غَسلَ يديهِ خرجَت من يديهِ كلُّ خطيئةٍ بطشَتها يداهُ معَ الماءِ – أو معَ آخرِ قَطرِ الماءِ فإذا غسَل رجلَيهِ خرجَت كلُّ خطيئةٍ مستها رِجلاهُ معَ الماءِ أو معَ آخرِ قطرِ الماءِ – حتَّى يخرُجَ نقيًّا منَ الذُّنوبِ

Atakapotawadha Mja wa Kiislam na kukosha Uso wake basi kila Dhambi aliyokua akiiangalia kwa Macho yake, huondoka kutokana na Maji hayo, kwa tone lake la mwisho au mithili yake, na atakapokosha mikono yake basi dhambi zote alizigusa kwa Mikono yake huyyondoka na Maji hayo au pamoja na tone la mwisho la maji hayo au mithili yake. Na atakapokosha Miguu yake basi dhambi zote ziliguswa na Miguu yake huyondoka kutokana na Maji hayo, au tone lake la mwisho au mithili yake. hadi Mtu huyo ni Msafi kabisa*.****(Sahih Muslim)***

*N*a amesema Imam At Tirmidhii kua;

النبي صلى الله عليه وآله وسلم قال: «إِذَا تَوَضَّأَ الْمُسْلِمُ ذَهَبَ الإِثْمُ مِنْ سَمْعِهِ وَبَصَرِهِ وَيَدَيْهِ وَرِجْلَيْهِ».

Amesema *Nabiyyu Salallahu Alayhi wa Salam* kua; Wakati Muislam anapotia Udhu basi Dhambi zake hua zinafutika kutoka kwenye Masikio yake, Macho yake, Mikono yake na Miguu yake.

Na akasema tena kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumwambia Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua:

يَا بُنَيَّ، إِنِ اسْتَطَعْتَ أَلَّا تَبِيتَ إِلَّا عَلَى وَضُوءٍ فَافْعَلْ، فَإِنَّهُ مَنْ أَتَاهُ الْمَوْتُ وَهُوَ عَلَى وَضُوءٍ؛ أُعْطِيَ الشَّهَادَةَ.

Ewe Mtoto wangu! Kama Unaweza basi usiende kulala Kitandani isipokua unapokua katika hali ya kua na Udhu, kwani yeyote yule atakaefariki huku akiwa katia hali ya Udhu basi Hufariki huku akiwa Shahidi.

Na anasema Imam An Nasai kua:

عن أي حازم قال: كنتُ خلفَ أبي هريرةَ وَهوَ يتوضَّأُ للصَّلاةِ ، وَكانَ يغسلُ يدَيهِ حتَّى يبلغَ إبطيهِ - فقلتُ يا أبا هريرةَ ما هذا الوضوءُ فقالَ لي : يا بني فرُّوخَ ! أنتُم ها هنا ؟ لَو علمتُ أنَّكم ها هنا ما تَوضَّأتُ هذا الوُضُوءَ سمعتُ خليلي صلَّى اللهُ عليهِ وسلَّمَ يقولُ : تبلغُ حليةُ المؤمنِ حيثُ يبلغُ الوضوءُ

Kutoka kwa Abi Hazim ambae amesema kua Mimi nilikua nyuma ya Abu Hurayrah wakati alipokua akitia Udhuy kwa ajili ya Sala. Na alikua akikosha mikono yake hadi kufikia kwenye kwapa zake. Hivyo name nikasema: 'Ya Abu Hurayrah ndio Udhuyu wa aina gani huo?'

Ambapo nae akasema: 'Ewe Banu Faruk, kumbe upoa hapa, hakika kama mimi ningekua nnajua kua uko hapa basi nisingetia Udhu huu, Nimemsikia Rafiki yangu *Salallahuu Alayhi wa Salam* akisema kua: 'Mapambo ya Muumini yatamfikia hadi juu katika sehemu zizlizoguswa na Udhuyu wake''

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua;

حدثنا أبو العلاء الحسن بن سوار حدثنا ليث -يعني الليث بن سعد - عن معاوية -هو معاوية بن صالح - عن أبي عثمان عن جبير بن نفير وربيعة بن يزيد عن أبي إدريس الخولاني وعبد الوهاب بن بخت عن الليث بن سليم الجهني، كلهم يحدث عن عقبة بن عامر قال: قال عقبة: (كنا نخدم أنفسنا، وكنا نتداول رعية الإبل بيننا فأصابني رعية الإبل فروحتها بعشي، فأدركت رسول الله صلى الله عليه وسلم وهو قائم يحدث الناس، فأدركت من حديثه وهو يقول: ما منكم من أحد يتوضأ فيسبغ الوضوء ثم يقوم فيركع ركعتين يقبل عليهما بقلبه ووجهه إلا وجبت له الجنة وغفر له، قال: فقلت: ما أجود هذا! قال: فقال قائل بين يدي: التي كان قبلها يا عقبة! أجود منها، فنظرت فإذا عمر بن الخطاب، قال: فقلت: وما هي يا أبا حفص؟ قال: إنه قال قبل أن تأتي: ما منكم من أحد يتوضأ فيسبغ

الوضوء، ثم يقول: أشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له، وأن محمداً عبده ورسوله إلا فتحت له أبواب الجنة الثمانية يدخل من أيها شاء).

Amesema Abu Aala Hasan Ibn Suwar kua amesema Al Layth Ibn Saad kua amesema Muawwiyah Ibn Salih kua amesema Abu Uthman kua amesema Jubayr Ibn Nufayr kua amesema Rabia Ibn Yazid kua amesema Abu Idris Al Khawlani kua amesema Abd Al Wahid Ibn Bakht kua amesema Layth Ibn Salim Al Juhan kua amesema Uqbah Ibn Amir *Radhi Allahu Anhu*kua:

'Sisi tulikua tunajihudumia Chakula na huku tukibadilishana zamu kuangalia Ngamia miongoni mwetu.

Hivyo ilipofika zamu yangu mimi kuwaangalia Ngamia ikawa ni Jioni na nikakutana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati akiwa amesimama na kuzungumza na watu na nikasikia Hadith aliyokua akiizungumzia kwa kusema kua: 'Hakuna hata mmoja miongoni mwenu atakaetia Udhu kikamilifu, na kisha akasimama na kusali Rakaa mbili akiwa na Ikhalsi ndani ya Moyo wake ndani ya Rakaa zake hizo. 'Isipokua Pepo hua ni Wajib kwa ajili ya Mtu huyo Na husamehewa Dhambi zake.'

Uqbah anaendelea kusema: Hivyo mimi nikasema: 'Hili ni habari nzuri sana'.

Na kisha mmoja kati ya watu waliokua mbele yangu ambae alikuwepo kabla akasema: 'Ewe Uqbah kuna Habari nzuri sana zaidi ya hio.'

Hivyo nami nikaangalia na nikamuona Umar Ibn Al Khattab na nikamuuliza: 'Ni hivyo kweli ya Abu Hafs?.'

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: Naam, kabla ya kuja kwako basi Alisema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hakuna hata mmoja miongoni mwenu atakaetia Udhu kikamilifu na kisha akasema: *'Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammada Aabduhu wa Rasuluhu.'*

Isipokua Milango minane ya Pepo hufunguliwa kwa ajili yake na kisha yeye ataweza kuingia katika Mlango wowote autakao.'*(Musnad Imam Ahmad)*

Na kwa upande wa Imam Muslim Ibn Hajjaj basi nae pia ameinukuu Hadith hii kama ilivyo. Na kisha pia akanukuu hadith nyegineyo yenye Mnyororo wa Sanad tofauti na wa Sanad ya Hadith hii, na hivyo hadith hio kua ni yenye kuongezeka maneno ya Dua ambayo ilikua kama ifuatavyo:

عن عمر بن الخطاب، قال

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم

من توضأ فأحسن الوضوء ثم قال "

أشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له وأشهد أن محمدا عبده ورسوله

اللهم اجعلني من التوابين واجعلني من المتطهرين

" فتحت له ثمانية أبواب الجنة يدخل من أيها شاء

الترمذي كتاب الطهارة عن رسول الله صلى الله عليه وسلم

Amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua:Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammada Aabduhu wa Rasuluhu.'*

Na kisha akasema: '*Allahuma JaAalni Mina Al Tawwabina wa Ja'Alani mina al Mutattahirina* - Ewe Allah Nijaalie mimi kua ni Miongoni mwa wenye Kutubu, Na nijalie kuani Miongoni mwa WaliotahirikaIsipokua Milango minane ya Pepo hufunguliwa kwa ajili yake na kisha yeye ataweza kuingia katika Mlango wowote autakao.'*(Sahih Muslim, Sunnan Abu Daud, Sunnan Ibn Majah,Sunnan An Nasai)*

Na hadith hii pia imenukuliwa na Imam At Tirmidhi katika Sahih At Tirmidhii.Hivyo ni meinukuu hadith hii kwa sababu hii Dua ya Mwisho ya Allahuma JaAlni Minna Al Tawwabina wa Ja'Alni Minna Al Mutattahirina ndio ambayo wengi sana huitumia, kuliko dua Nyengine zote.Mbali ya kua Dua isemayo;

اللهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي

وَوَسِّعْ لِي فِي دَارِي

وَبَارِكْ لِي فِي رِزْقِي

Allahumaghfirly Dhanbi -Ya Allah Nisamehe Dhambi zangu.
Wa waassi'ly Fi Darri - Na Nipanulie Makazi yangu.
Wa Barikly Fi Rizqy - Na Nibariki katika Riziki yangu.

Ambayo imenukuliwa na Imam An Nawawi, Imam Ibn Al Qayyim, Imam Ibn Mulaqin kutoka kwenye Musnad Imam Ahmad, Musnad Imam Abu Yaala, Musannaf Ibn Abi Shaybah,Al Duaa ya Imam At Tabrani n.k, kutoka kwa Sahaba Abu Musa Al Ashari Radhi Allahu Anhu ambae amesema kua:

أَتَيْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِوَضُوءٍ ، فَتَوَضَّأَ ، وَصَلَّى ، وَقَالَ: اللهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي ، وَوَسِّعْ لِي فِي دَارِي ، وَبَارِكْ لِي فِي رِزْقِي

Nilimpelekea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Maji ya Kutia Udhu Hivyo nae akatia Udhu na kisha na kisha akasema:

Allahumaghfirly Dhanbi -Ya Allah Nisamehe Dhambi zangu.
Wawassi'ly Fi Darri - Na Nipanulie Makazi yangu.
Wa Barikly Fi Rizqy - Na Nibariki katika Riziki yangu.

Ambapo Imam Al Muhaqqiqin Al Faqih Imam Ibn Hajar Al Haythami Al Makki Al Shafii ameiweka hadith hii kwenye Mlango wa Kile kinachotakiwa kusemwa baada ya Kutia Udhu, na hivyo hivyo pia Imam Al Ramli katika *Nihayat Al Muhtaj* na Imam Al ManawiKatika *Fat-h Al Qadir*, Imam Ibn Al Qayyim katika *Zadd Al Maad*, Imam An Nawawi katika *Al Adhka*r n.k

Ambapo Wanazuoni wanasema kua Dua hii ni Dua ambayo nzuri sana kusoma Kabla ya Kutia Udhu, baada ya kutia Udhu, Ndani ya Sala na nje ya Sala pia na hii ni kwa sababu Dua hii haikuacha kitu ndani yake. Kwani anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

أَنَّ رَجُلاً قَالَ: يَا رَسُولَ اللهِ سَمِعْتُ دُعَاءَكَ اللَّيْلَةَ ، فَكَانَ الَّذِي وَصَلَ إِلَيَّ مِنْهُ أَنَّكَ تَقُولُ:" اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي ، وَوَسِّعْ لِي فِي دَارِي ، وَبَارِكْ لِي فِيمَا رَزَقْتَنِي " قَالَ: فَهَلْ تَرَاهُنَّ تَرَكْنَ شَيْئًا.

Kuna Mtu alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kusema: Ya Rasul Allah! Hakika Jana usiku mimi niliisikia Dua yako isemayo:Allahuma ighfirly Dhanbi, Wa wassil'i fi Darri wa Barikly fi Rizqi. (Ya Allah Nisamehe Dhambi Zangu, Nipanulie Makazi yangu na Nibariki katika Riziki zangu.)Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Hivi Jee unadhania kua Dua hii imeacha kitu chochote Ndani yake?*(Imam At Tirmidhi)*

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua Haikuacha kitu kwa sababu tunapoiangalia Maana yake basi tunaona kua inasema:

اللهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي

وَوَسِّعْ لِي فِي دَارِي ،

وَبَارِكْ لِي فِي رِزْقِي

Ya Allah Usiyajali Madhambi yangu na Usiniadhibu kutokana nayo.
Ya Allah Nipanulie Makazi yangu kwa Kunijazia Rehma zako hapa Duniani, Kaburini na Siku ya Malipo.
Ya Allah Niongezee Baraka katika Ulichonijaalia kukipata na niwe ni mwenye Kukinai na Kuridhika nacho.
Aamin.

Ambapo amesema Imam Abd Al Baqiy Ibn Yusuf Ibn Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ulwan Al Zarqani Al Maliki kuhusiana na Dua hio Isemayo:

اللهُمَّ اغْفِرْ لِي ذَنْبِي

وَوَسِّعْ لِي فِي دَارِي ،

وَبَارِكْ لِي فِي رِزْقِي

Kua Ni Bora Kuisoma Dua hii Wakati Unatia Udhu na pia baada ya Kutia Udhu.'*(Sharh Mukhtasar Al Khalil)*Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Abd Al Haqq Al Shibli katika Ahkam Al Kubra.

Ama kwa Upande wa Imam Abu Qasim Sulayman Ibn AhmadIbn Ayyub Ibn Muttayyir Al Lakhmi Ash Shami At Tabarani kuhusiana nayo kua: '**Hii ni Dua nzuri Kuisoma baada ya Sala** (Al Awsat)

Na akasema Imam Al Shawkani kua: '**Hii ni Hadith yenye Dua ya kwenye Sala, Dua ya Kwenye Kutia Udhu, n.k.'***(Tuhfah Dhakiriina)*

Ambapo imesemaa kwenye Fiqh Al Adiyah Al Al Adhkar kuhusiana nayo kua: '***Allahuma Ighfirly Dhanbi* maana yake hua ni Kuomba Msamaha wa kila kosa lililokosewa, kila kasoro iliyopunguza kinachotakiwa kukamilishwa. Kwani Kusamehewa Dhambi ndio Msingi wa Kila Jema Katika Maisha ya Duniani na Akhera**. **Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿وَأَنِ ٱسْتَغْفِرُواْ رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوٓاْ إِلَيْهِ يُمَتِّعْكُم مَّتَاعاً حَسَناً إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِى فَضْلٍ فَضْلَهُ وَإِن تَوَلَّوْاْ فَإِنِّيٓ أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيرٍ﴾

Waani istaghfiroo rabbakum thumma tooboo ilayhi yumattiAAkum mataAAan hasanan ila ajalin musamman wayu/ti kulla dhee fadhlin fadhlahu wa-in tawallaw fa-inee akhafu AAalaykum AAadhaba yawmin kabeerin*(Surat Hud 11:3)*

*Tafsir:**Na (Anakuamrisheni) Muombe Msamaha kwa Mola wenuNa Kisha Tubuni kwa Kurudi kwake Ili akujaalieni Starehe Nzuri SanaKwa Kipindi Maalum kilichochaguliwaNa yeye Humpa Kila Mwenye Fadhila, Fadhila Zake. Lakini Kama Mkigeuka na Kumpa mgongoBasi kwa Hakika Mimi Nnakukhofieni Juu yenu Adhabu Ya Siku Kubwa Sana ya Kufufuliwa.***

Na hivyo kutokana na Maneno hayo basi ndio ikawa bora ya Kuomba Msamaha kua ni kwenye Kufuatiwa na Upana wa Makazi na Ongezeko la Riziki katika Dua hii.

Kwani kuomba kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Kuongezewa Upana wa Makazi kunamaanisha Upana wa Makazi ya Kidunia kwani Ukubwa wa Nyumba ndio Wingi wa Furaha ya Kidunia.

Na pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimaanisha Upana wa Makazi ya Kaburini kwani Kaburi ndio *Darr Al Haqiiqiyyah* (Makazi ya Hakika).

Na vile vile inaweza ikawa amekusudia Pepo kwani ndio sehemu ya Makazi ya Milele na Starehe zisizokua na Mwisho. Hivyo Maneno haya Yanajumuisha Makazi yote haya.

Na Kuomba kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuaAongezewe Baraka kwenye Riziki ndani ya Dua hii kunamaanisha kuomba Kutiliwa Baraka katika Riziki yake kunakojaa wema.

Kwani neno Barakah hua linamaanisha *Thabatuh wa Ziyaddah* (Uthibitisha wa Kubakiwa na Ulichoruzukiwa bila kupingukiwa na kuongezeka kwake ulichoruzukiwa.'(*Fiqh Al Adiyah Al Adhkar)*

Na amesema Imam Ibn Hibban kua:

عَنْ سَعْدِ بْنِ أَبِي وَقَّاصٍ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَرْبَعٌ مِنَ السَّعَادَةِ الْمَرْأَةُ الصَّالِحَةُ

وَالْمَسْكَنُ الْوَاسِعُ وَالْجَارُ الصَّالِحُ وَالْمَرْكَبُ الْهَنِيءُ وَأَرْبَعٌ مِنَ الشَّقَاوَةِ الْجَارُ السُّوءُ وَالْمَرْأَةُ السُّوءُ وَالْمَسْكَنُ الضِّيقُ وَالْمَرْكَبُ السُّوءُ

Amesema Said Ibn Abi Waqqas *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua: mambo manne hua ni sehemu Furaha ambayo ni: Mke mwema, Makaazi yenye nafasi kubwa, Jirani Mzuri na Kipando Kizuri. Na mambo manne ni sehemu ya huzuni ambayo ni: Jirani Mbaya, Mke Muovu, Makaazi yasiyokua na sehemu kubwa na kipando kibaya.

Ambapo kwa upande wa Sahaba Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allah Anhu* basi yeye amesema kua : **'Yeyote yule atakaefanya ovu basi atakua na malipo ya ovu moja kwenye kitabu chake, na aakaefanya jema basi ataandikiwa mema kumi ndai ya kitabu chake, hivyo kama mtu akiadhibiwa kwa uovu wake katika Dunia hii, basi hua ni mwenye kubakiwa na mema kumi kati ya aliyoyafanya. Na akama ikiwa hakuadhibiwa basi hua ni mwenye kubakiwa na tisa kutokana na kumi kwani moja litafutwa katika siku ya malipo, kwa maana hio basi: 'Ameangamia yule ambae mamoja yake yatayazidi mamia yake''***(Imam Ibn Jarir)***

Na amesema Imam Al Hafidh Al Mubarakpuri kua: **'Maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yasemayo kua;**

فَهَلْ تَرَاهُنَّ تَرَكْنَ شَيْئًا

Hivi Jee imeacha Kitu chochote Kile?

Ni yenye kumaanisha kua Dua hii imejmuisha kila kilicho cha kheri hapa Duniani na Akhera.'*(Tuhfah Al Ahwadhi)*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Al Ghazali Al Thani Sultan Al Mutakallimin Imam Al Mushaqqiqin Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kuhusiana na aya hii

﴿وَأَنِ ٱسْتَغْفِرُواْ رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوٓاْ إِلَيْهِ يُمَتِّعْكُم مَّتَاعاً حَسَناً إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِى فَضْلٍ فَضْلَهُ وَإِن تَوَلَّوْاْ فَإِنِّيٓ أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيرٍ﴾

Waani istaghfiroo rabbakum thumma tooboo ilayhi yumattiAAkum mataAAan hasanan ila ajalin musamman wayu/ti kulla dhee fadhlin fadhlahu wa-in tawallaw fa-inee akhafu AAalaykum AAadhaba yawmin kabeerin*(Surat Hud 11:3)*

*Tafsir: **Na (Anakuamrisheni) Muombe Msamaha kwa Mola wenu Na Kisha Tubuni kwa Kurudi kwake na Akujaalieni Starehe Nzuri Sana Kwa Kipindi Maalum kilichichaguliwa Na yeye Humpa Kila Mwenye Fadhila, Fadhila Zake Lakini Kama Mkigeuka na Kumpa mgongo Basi kwa Hakika Mimi Nnakukhofieni Juu yenu Adhabu Ya Siku Kubwa Sana ya Kufufuliwa.***

Kua: Hivi Jee hakusema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Dunia hii ni kama Jela kwa Muumini na ni kama Pepo kwa Asiekua Muumini?''

Halafu hapo hapo tunaona kua wale wenye kujaribiwa zaidi kwa Mitihani miongoni mwa Watu ni Mitume, na wale waliokua karibu yao na walio karibu yao? Hivyo Jee inakuaje Aya hii inasema kua Mkiomba Msamaha na Kurudi kwake basi atakujaalieni Raha na starehe kwa mda maalum?

Hivyo Jibu la Suali hili ni kua: 'Mwenye kukipenda kituhua hawezi kuachana nacho kwani hujihisi kua na raha pale anapokua na kitu akipendacho.

Hivyo kutokana na kua Muumini hua ni mwenye Kumpenda *Allah Subhanah wa Taala,* basi Muumini huyo hua ni mwenye kuachana na kila kitu kilichokua mbali na *Allah Subhanah wa Ta'ala* yaani Dunia, na hivyo Dunia hua si kitu chenye thamani kwake, hivyo kila anapozidi kua mbali nayo basi ndio anavyozidi kua na ukaribu na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kuzidi kua na hisia za Raha na Furaha ndani ya Moyo wake.

Ama kwa upande wa yule mwenye kuipendelea Dunia hui basi hua ni wenye kuweza kumiliki Mali za Dunia, ambazo kamwe hua hawezi kutabiri ni lini na wakati gani atapokonywa Mali hizo,au lini atakumbwa na Mauti.

Hivyo watu hawa hua ni wenye kua katika hali ya kujawa na khofu na wasiwasi ndani ya Nyoyo zao na kukosa utulivu ambapo hua ni kama wenye kumwagiwa Maji yabaridi kwenye kwenye Raha na Starehe zao.

Na hivyo kutokana na Mwenye Imani kua ni mwenye kua ndani ya Mipaka ya vitendo vyake basi hua si mwenye Kua na khofu wala wasiwasi na hivyo Furaha yao haipungui.

Ambapo tunapozungumzia neno Dhu Al Fadhl yaani Wenye Kua na Fadhila au waliofadhiliwa basi hapa hua ni Wale waliokua na ari na Ikhlasi katika kutekeleza Majukumu yao Kiibada na kuongezea ziada.

Naam.. Hivyo kwa upande wa Wenye Fadhila basi hua ni wale waliofadhilishwa na *Allah Subhanah wa Ta'al*a na kisha Wakajijua kua wamepewa fadhila kutoka kwa Mola wao, na hivyo wakafanya mema na wakazidisha ziada katika mema hayo na wakafanya Istighfar kwa wingi hivyo malipo yao hua ni kufadhiliwa zaidi kimalipo na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Miongoni mwa njia za kuzipata Fadhila za Allah Subhanah wa Ta'ala ni kama ilivyoainishwa kwenye aya zifuatazo:

﴿يَآ أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَأْكُلُواْ ٱلرِّبَا أَضْعَافاً مُّضَاعَفَةً وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ۞ وَٱتَّقُواْ ٱلنَّارَ ٱلَّتِيۤ أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ۞ وَأَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ۞ وَسَارِعُوۤاْ إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا ٱلسَّمَاوَاتُ وَٱلأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ۞ٱلَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّآءِ وَٱلضَّرَّآءِ وَٱلْكَاظِمِينَ ٱلْغَيْظَ وَٱلْعَافِينَ عَنِ ٱلنَّاسِ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلْمُحْسِنِينَ ۞وَٱلَّذِينَ إِذَا فَعَلُواْ فَاحِشَةً أَوْ ظَلَمُوۤاْ أَنْفُسَهُمْ ذَكَرُواْ ٱللَّهَ فَٱسْتَغْفَرُواْ لِذُنُوبِهِمْ وَمَنْ يَغْفِرُ ٱلذُّنُوبَ إِلاَّ ٱللَّهُ وَلَمْ يُصِرُّواْ عَلَىٰ مَا فَعَلُواْ وَهُمْ يَعْلَمُونَ۞ أُوْلَئِكَ جَزَآؤُهُمْ مَّغْفِرَةٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ وَجَنَّاتٌ تَجْرِى مِنْ تَحْتِهَا ٱلأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَنِعْمَ أَجْرُ ٱلْعَامِلِينَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo la ta/kuloo alrriba adAAafan mudaAAafatan waittaqoo Allaha laAAallakum tuflihoona; Waittaqoo alnnara allatee oAAiddat lilkafireena; WaateeAAoo Allaha waalrrasoola laAAallakum turhamoona; WasariAAoo ila maghfiratin min rabbikum wajannatin AAardhuha alssamawatu waal-ardhu oAAiddat lilmuttaqeena; Alladheena yunfiqoona fee alssarra-i waalddarra-i waalkadhimeena alghaythaa waalAAafeena AAani alnnasi waAllahu yuhibbu almuhsineena; Waalladheena itha faAAaloo fahishatan aw thalamoo anfusahum thakaroo Allaha faistaghfaroo lithunoobihim waman yaghfiru aldhdhunooba illa Allahu walam yusirroo AAala ma faAAaloo wahum yaAAlamoona Ola-ika jazaohum maghfiratun min rabbihim wajannatun tajree min tahtiha al-anharu khalideena feeha waniAAma ajru alAAamileena ;*(Surat Al Imran 3:130-138)***

Tafsir: ***Enyi Wale ambao Mmeamini, Msile Riba iliyoongezeka na kuzidishika, bali Muogopeni Allah Subhanah wa Ta'ala ili mpate kua wenye kufuzu. Mtiini Allah na Mtume wake Salallahuyu Alayhi wa Salam ili mpate kurehemeka. Na Kimbilieni katika njia yenye Msamaha wa Mola wenu, na Pepo ambayo upana wake kama Upana wa Mbingu na Ardhi ambayo imetayarishwa na Wenye Kufanya Mema. Wale ambao ni wenye kutoa kwa Ajili ya Allah Subhanah wa Taala katika wakatiwa Neema na Mitihani, na wanaozikandamiza Hasira zao na wanao wasamehewe watu. Kwani kwa hakika Allah ni mwenye kuwapenda wenye kufanya Mema. Na wale waliofanya Madhambi za matamanio ya Nafsi zao au kua ni weny ekujidhuylumu nafis zao kwa maovu na kisha wakamumbuka Allah Subanah wa Ta'ala na kuomba awasamehe Dhambi zao. Na hakuna anaeweza kusamehe Dhambi isipokua Allah Subhanah wa Ta'ala. Na wakawa hawakudumu kweny dhambi hizo huku wakiwa wanajua waliyoyafanya. Malipo yao wat hao ni Kusamehewa na Mola wao na Pepo zenye Mabustani na Mito yenye kutiririka Maji ndani yake. Watakaa ndani yake milele. Ni malipo makubwa kiasi gani hayo kwa wenye kufanya Mema.***

Hivyo bila ya shaka wenye kujua kuhusiana na Fadhila za Mola wao hua ni wenye kujitahidi kutafuta njia ya kupata fadhila zaid na hivyo hua ni wenye kudumu na Istighfar na kudumu na Udhu wao kutokana na kutopenda kubatilisha Ibada zao, kwani batilisho huwabatilishia Fadhila kutoka kwa Mola wao na huendelea kufanya Istighfar kutokana na kasoro zao kiibada na katika amali zao. Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* pia kua:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ ٱلْمُتَطَهِّرِينَ﴾

Inna Allaha yuhibbu alttawwabeena wayuhibbu almutatahhireena *(Surat Al Baqara 2:222)*

*Tafsir:K****wani kwa hakika Allah anawapenda wenye kufanya toba na wenye kujitoharisha.''***

Hivyo kulingana na maana ya aya yetu iliyosema:

﴿وَيُؤْتِ كُلَّ ذِى فَضْلٍ فَضْلَهُ﴾

Wayu/ti kulla dhee fadhlin fadhlahu *(Surat Hud 11:3)*

Tafsir: **Na yeye Humpa Kila Mwenye Fadhila Fadhila Zake**.

Basi tunaona kua *Dhu Al Fadhli* hua ni wale wenye Kua na Ari na Ikhlasi Katika Kutekeleza Majukumu yao Kiibada kwa wingi zaidi.Ambapo kwao wao watu hawa basi Hali ya Kudumu na Kutofisidi Udhu wao hua ni hali inayowafanya kujihisi kua katika Mazingira ya Kiimani zaid ambako huwapelekea kukaa mbali na Maovu.Kwani Udhu hua ni wenye kumfanya Mtu kua na Umakini katika Vitendo vyake na uhusiano wake na Mola wake, na hivyo kua na Utayari wa kujitolea kuwasiliana nae Mola wake ndani ya wakati wowote wakati yupo na Udhu wake.

Hivyo Udhu ni Kitu chenye Umuhimu Mkubwa sana katika Dini ya Kiislam kwani ndio Kitu kinachoainisha Usafi wa Kinafsi na Kiwiliwili.Na ni Muhimu sana kwa Kila Muislam Kujua Juu ya Kua nao na juu ya Kubatilika kwake.Hivyo tunapozungumzia kuhusiana na yanayobatilisha Udhu basi yapo kadhaa ikiwemo Hadath.

Ambapo anasema Al Qadhi, Al Faqih Al Zahid Al Allamah Imam Abu Tayyib Abu Shujaa Shihab Ad Din Ahmad Ibn Al Husayn Ibn Ahmad Al Isfahani Al Shafii kua: **‘Kuna Sababu 5 ambazo humpelekea Mtu kua ni Mwenye Kua na Hadath ambazo ni:**

1-Kutokwa na Kitu katika moja kati ya Tupu mbili, ambazo ni tupu ya mbele ya Haja Ndogo na Tupu ya Nyuma ya Haja kubwa.

2-Kulala Usingizi huku Makalio yakiwa hayajagusana na kitu madhbuti chini yake.

3-Kupotewa na Fahamu kutokana na Kilevi au Maradhi.

4-Kugusana na Mtu wa Jinsia Nyengine yaani kwa Mwanamme mwenye UdhuKugusana na Wanawake au kwa Mwanammke mwenye Udhu kugusana na Mwanamme.

5-Kugusa au Kushika Sehemu za Siri kwa kutumia Tumbo la Viganja vya Mikono.*(Matn Al Ghayah wa Al Taqrib)*

Ambapo mbali ya Hadath basi miongoni mwa yanayobatilisha Udhu hua ni pamoja na:

6-Kua na Shaka juu ya kua na Udhu ama la.

7-Kuritad au Kutoka katika Uislam.

Na Imam Ibn Battal anasema: “**Matukio ambayo wanazuuoni wamekubaliana yanabatilisha wudhuu, zaidi ya yale aliyoyataja Abu Hurairah: mkojo, kinyesi, maji ya kabla ya kumwaga manii, shahawa, kujamiiana, kupoteza akili kwa namna yoyote ile, na usingizi wa kupindukia.*”(Mawsuah Fiqhiyyah)***

Naam haya ni baadhi ya mambo ambayo yatakapomtokea Mtu husika basi hua ni yenye kumpelekea Mtu kua ni mwenye kubatilishika Udhu wake.

Naanasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Shara An Nawawi Al Shafii kua: **‘Kama Ikitokea kwa Mtu ambae ni mwenye Kufanya Ibada ya Sala na Udhu aake ukabatilika kwa kutokana na Hadath wakati akiwa ndani ya Sala basi Wanazuoni Wanakubaliana kua Sala ya Mtu Husika Hubatilika Hapo hapo. Na Juu ya Hili basi Wanazuoni wanakubaliana kua kubatilika huko kwa Sala hua wala hakutegemeani na hali ya kua kama Mtu huyo ameubatilisha Udhu wake kwa Makusudi ama la, wala kua Mtu husika hakujua kua juu yuko ndani ya Sala ama la.**

Na Wanazuoni wanakubaliana kua haijaalishi kua kama ikiwa Mtu alipatwa na Hadath hio kutokana na Kitendo kitokanacho na yeye mwenyewe ama kitokanacho na Mtu mwengine au alikua na Hadath kabla ya Udhu ama la.

Hivyo Udhu wa Mtu husika hubatilika kutokana na Hadath hio na hii hakuna kutokukubaliana juu yake.'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na kutokana na Kubatilika kwa udhu huo basi Sala ya Mtu husika Hubatilika kwa sababu ya kama alivyosema tena Shaykh Ul Islami Imam An Nawawi kua:**'Kama Ikiwa Moja kati ya sharti ya Sala itakua limebatilika, kama vile Kua Tohara na Udhu, Kujihifadhi Kimavazi n.k basi na Sala husika pia hubatilika.**'*(Al Majmu Sharh Al Muhadhdhab)*

Kwani kuna baadhi yetu wanaweza wakajiuliza suali la kua: Kama Itakua Mtu anasali kwenye Sala ya Jamaa na yuko kwenye Safu na kisha Udhu ukamtoka kwa njia Moja au Nyengine. Jee anatakiwa afanyeje?

Naam, Jibu la Suali hili tunalipata moja kwa moja kutoka kwa *Habib Allah Al Mustafa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae ametufundisha juu ya hili pale aliposema katika Hadith kua:

إذا قطع شرطا من شروطها كالطهارة و الستارة و غيرها بطلت صلاته

Kama Itatokea Mmoja wenu Atapatwa na Hadath wakati akiwa ndani ya Sala, basi na ashike Pua na Kisha Ageuke na kutoka ndani ya Safu ya Sala*(Sunan Abu Daud)*

Naam..huu ndio Ushauri aliotoa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa Mtu atakaekua na Hadath na hivyo Udhu wake kutenguka na kupelekea kufisidika kwa Sala yake.Hivyo Mtu husika hutakiwa kushika Pua yake na kutoka haraka sana nje ya Safu na nje ya Sala,

Ambapo Hikma iliyomo ndani yake tukio hili la kushika Pua na kutoka ndani ya Safu hua ni kuficha aibu yake Mtu husika kwani watu watadhania kua ametoka ndani ya Sala kwa sababu ya kua na Matatizo ya Pua kua inatoka Damu. Kwani anasema Imam Al Munawi Al Shafii kua:

Mtu aliekua na Hadath ndani ya Sala basi na Ashike Pua yake kama kwamba anatokaa na Damu Puani. Na kisha atoke Nje ya Safu na Kuachana na Sala yake na kisha Akajitoharishe na kutia Udhu upya na kisha ndio Arudi tena Kusali Upya.

Na hii ni kwa sababu Mtu atakaekua na Hadath atakua ni mwenye Kuona Aibu pale wenzake wakiwa wanajua kua Mtu huyo ametoka kwa sababu ya Hadath. Na hivyo kitendo cha Kushika Pua hua ni chenye kumfichia Aibu yake na Kumuondolea Fedheha pale anapotoka kwenye Safu ya Sala.

Na ndani ya Ushauri huu kuna Hikma ya Kuficha kitu kinachofedhehesha kwa kuonesha kitu chengine badala yake ambacho hua si Riyah.

Bali hua ni kuonesha Kitu kizuri na kijiokoa kutokana na fedheha na pia Kumhifadhi mhusika kutokana na kusengenywa na wengine.*(Al Faidh Al Qadir Sharh Jamii Al Saghir)*

Hivyo Mtu anapofikwa na hali kama hii ya kubatilika kwa Udhu wakati akiwa ndani ya Safu ya Sala ya Jamaa basi anatakiwa akatishe Sala hapo hapo.

Kisha Ashike Pua yake ili Watu wamuone kua Amtoka kwenye Sala kwa Sababu ya Damu ya Pua na sala si kwa sababu ya Kutenguka kwa Udhu wa kwa njia moja au nyengine.Na hivyo kua ni mwenye Kutoka Nje ya Sala huku akiwa ni mwenye Kulinda Heshima yake.

Na baadhi miongoni mwetu wanaweza wakajiuliza suali lifuatalo: Hivi kwa nini katika Kunuu hua sinukuu kutoka katika Kitabu cha Fiqh Sunnah cha Shaykh Said Sabiq? Naam..hili ni Suali zuri sana ambalo thamani yake ni zaidi ya Milioni tano.

Na nnasema hivi kwa sababu Ni Kweli Kitabu cha Fiqh Al Sunnah cha Shaykh Said Sabbiq ni Kitabu Maarufu sana katika Karne yetu kwani Shaykh Said Sabbiq mwenyewe amefariki mwaka 2000. Na Kitabu chake cha Fiqh Sunnah ambacho kimechanganya Mitizamo mbali mbali ya Fiqh, kwa kutumia Vithibitisho vya Hadith ambazo Sanad zake zimefupishwa.

Hivyo ingawa ni Kitabu ambacho kimefanyiwa Jitihada katika maandalizi yake lakini hapo hapo ni kitabu ambacho hakiwezi kutegemewa kwa Wenye Kutafuta Ilm na wasiojua Kitu chochote.Kwa sababu ya kua Fiqh Sunnah ni Kitabu ambacho Kina kasoro kadhaa katika kuelezea Mitizamo ya Fiqh ya Skuli za Madhhab na hivyo kutoweka wazi usahihi wake.

Jambo ambalo humpelekea Mtu asiekua na Ilm kuweza kuchanganyikiwa kutokana na Mitizamo iliyomo ndani yake.Na hivyo kuwapelekea watu kufanya Talfiq yaani kuchanganya Mitizamo tofauti katika Ibada moja, jambo ambalo hupelekea kubatilika kwa Ibada husika.Na juu ya Suali la Talfiq katika Ibada moja basi Wanazuoni wanakubaliana kua Kunabatilisha Ibada husika.

Ama kwa watakaotaka kujua zaidi kuhusiana na Talfiq basi na watafute kitabu cha Al Mustakshif Abu Manal Danah kiitwacho Ijtihad na Taqlid Historia ya Maimamu na Madhhab yao katika Uislam. Ambacho kinapatikana bure Mtandaoni.

Mbali ya hivyo lakini pia Kitabu cha Fiqh Al Sunnah ni kitabu ambacho kina mitizamo inayopingana na Mitizamo ya Maimamu wa Madhhab, kiasi ya kua kuna baadhi ya Mitizamo iliyopewa kipaumbele zaidi ambayo hata hivyo Mitizamo hio si yenye kupewa kipaumbele na Maimamu wa Madhhab.

Hivyo Kitabu cha *Fiqh Al Sunnah* ingawa ni Kitabu cha Fiqh kama kinavyojieleza lakini hivyo hiki ni kitabu ambacho kinatakiwa kuepukwa, kwani ukikifuata basi kitakubatilishia baadhi ya Ibada zako. Ambapo hizini baadhi ya sababu ambazo zinatupelekea kua si wenye Kunukuu kutoka kwenye Kitabu hicho mbali ya kua Kitahu hicho kimempatia Shaykh Said Sabbiq Nishani ya Uandishi ya Mfalme Feisal wa Saudi Arabia kwa sababu ya Mitizamo iliyomo ndani yake, inayounga Mkono Kutofuata Maimamimu wa Madhhab. Jambao Ambalo mimi mwenyewe siliungi mkono na wanasema wenye kuua kua: '**Usitamke kwa Ulimi wako kile ambacho Moyo wako Unapingana Nacho.'**

Naam, hivyo anasema Imam At Tirmidhii kua:

حَدَّثَنَا قُتَيْبَةُ، حَدَّثَنَا عَبْدُ الْعَزِيزِ بْنُ مُحَمَّدٍ، عَنْ سُهَيْلِ بْنِ أَبِي صَالِحٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " إِذَا كَانَ أَحَدُكُمْ فِي الْمَسْجِدِ فَوَجَدَ رِيحًا بَيْنَ أَلْيَتَيْهِ فَلاَ يَخْرُجْ حَتَّى يَسْمَعَ صَوْتًا أَوْ يَجِدَ رِيحًا " . قَالَ وَفِي الْبَابِ عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ زَيْدٍ وَعَلِيِّ بْنِ طَلْقٍ وَعَائِشَةَ وَابْنِ

عَبَّاسٍ وَابْنِ مَسْعُودٍ وَأَبِي سَعِيدٍ . قَالَ أَبُو عِيسَى هَذَا حَدِيثٌ حَسَنٌ صَحِيحٌ . وَهُوَ قَوْلُ الْعُلَمَاءِ أَنْ لاَ يَجِبَ عَلَيْهِ الْوُضُوءُ إِلاَّ مِنْ حَدَثٍ يَسْمَعُ صَوْتًا أَوْ يَجِدُ رِيحًا . وَقَالَ عَبْدُ اللَّهِ بْنُ الْمُبَارَكِ إِذَا شَكَّ فِي الْحَدَثِ فَإِنَّهُ لاَ يَجِبُ عَلَيْهِ الْوُضُوءُ حَتَّى يَسْتَيْقِنَ اسْتِيقَانًا يَقْدِرُ أَنْ يَحْلِفَ عَلَيْهِ . وَقَالَ إِذَا خَرَجَ مِنْ قُبُلِ الْمَرْأَةِ الرِّيحُ وَجَبَ عَلَيْهَا الْوُضُوءُ . وَهُوَ قَوْلُ الشَّافِعِيِّ وَإِسْحَاقَ

Amesema Qutaybah kua amesema Abd Al Aziz Ibn Muhammad kua amesema Suhayl Ibn Abi Salihkua amesema Baba yake kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kama ikiwa mmoja wenu Yuko Msikitini akahisi Upepo baina ya Makalio yake basi asiondoke hadi Awe amesikia Sauti au Harufu Na pia Ibada nyenginezo.Ambapo anasema Imam Al Tirmidhii kuhusiana nayo Hadith hii kua: Hii ni Hadith Sahih, ambayo inathibitisha kua Kama Mtu atakutwa na hali hii basi Kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni ni kua:Mtu husika hatokua na Wajibu wa Kutia Udhu upya hadi pale atakaposikia Sauti ya Gesi hio au Harufu ya Gesi hio. Kiasi ya kua atakua ni mwenye kuweza kuapia juua yake. Na Kama Mwanammke atatokwa na Gesi au hewa katika sehemu za mbele za Siri basi hua ni lazima kwake kutia Udhu upya na huu ndio mtizamo wa Imam Al Shafii na Imam Is-haq Ibn Rahawayh. '*(Jamii Al Tirmidhii)***

Ambapo hii ni hadith Sahih ambayo pia imenukuliwa na Aisha R*adhi Allahu Anha*, Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu*,n.k.

Na tunaizungumzia Hadith hii kutokana na kua ni yenye kuthibitisha kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu kunakosababishwa na Kutoka kwa Gesi kupitia katika Utupu wa haja Kubwa, ambako nako husababisha kubatilika kwa Ibada ya Sala.

Ambapo amesema Imam Abd Allah Ibn Mubarak kua: '**Hata Kama itakua Mtu atakua na Shaka juu ya Udhu wake juu ya tokeo hili basi Udhu haitokua Wajibu Juu yake hadi atakapokua na Uhakika wa Kua Inambidi akatie Udhu**.'

Kwani kuna hadith isemayo:

حَدَّثَنَا إِسْحَاقُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ الْحَنْظَلِيُّ، قَالَ أَخْبَرَنَا عَبْدُ الرَّزَّاقِ، قَالَ أَخْبَرَنَا مَعْمَرٌ، عَنْ هَمَّامِ بْنِ مُنَبِّهٍ، أَنَّهُ سَمِعَ أَبَا هُرَيْرَةَ، يَقُولُ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " لاَ تُقْبَلُ صَلاَةُ مَنْ أَحْدَثَ حَتَّى يَتَوَضَّأَ ". قَالَ رَجُلٌ مِنْ حَضْرَمَوْتَ مَا الْحَدَثُ يَا أَبَا هُرَيْرَةَ قَالَ فُسَاءٌ أَوْ ضُرَاطٌ.

Amesema Is-haq Ibn Ibrahim Al Handhali kua amesema Abd Razaq kua amesma Ma'mar kua amesema Hammam Ibn Munabih kua amemsikia Abu *Hurayrah Radhi Allahu Anhu* akisema kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*: Sala ya Mtu ambae Umebatilika Udhu wake hua haikubaliwi hadi atakapotia Udhu upya na Kusali tena.

Ambapo Hamam Ibn Munabih anasema kua: Kuna Mtu kutoka Hadhramawt akamuuliza Abu Hurayrah*Radhi Allahu Anhu:* kwa kusema: Kubatilika Kwa Udhu ndio vipi?.

Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* akasema: FusaaUun aw Dhuratu -Kujamba au Kutokwa na Gesi*(Sahih Bukhari)*

Na kwa upande wa Imam Ibn Abidin Ash ShamiAl Hanafi basi amesema kua: **'Kama ikiwa Mtu hana uhakika kua ametokwa na gesi ama la, basi anatakiwa ajihesabu kua hakutokwa na kitu'***(Radd Mukhtar, na Imam Ibn Nujaym katika Al Ashbah)*

Na imesemwa katika Nayl Al Raja kua: '**Hakuna haja kwa mtu kujisafisha sehemu zake za Siri baada ya kutoa gesi, kwani kufanya hivyo hua ni Makruh kwa sababu Kutoa Gesi hua hakumfanyi Mtu awe Mchafu.'**

Na anasema Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: **'Kitu chochote kitakachotoka katika Tupu ya Mbele au ya Nyuma ya Mwanamme Au Mwanammke hua kinabatilisha Udhu**. **Iwe kitu hicho ni Choo kikubwa, Mkojo, Gesi, Upepo,Usaha, Minyoo, Damu, Vijiwe au kitu chengine chochote kile.**

Na hakuna utofauti juu ya hili wa kua Utokaji huo wa Kitu kua ni wa Mara kwa mara au ni wa Nadra.

Na hakuna autofauti kuhusiana na Utokwaji wa Gesi, Upepo au Hewa iwe katika Tupu ya Mbele au ya Nyuma iwe ya Mwanamme au ya Mwanammke.

Na juu ya hili amezungumzia Imam Al Shafii katika Al Umm na pia wamezungumzia As-hab Al Wujuh wa Madhhab yetu kwa kukubaliana.'*(Al Majmuu)*

Ambapo maneno hayo hayo ndio pia aliyoyasema Shaykh Ul Islami, Imam Al Muhaqqiqin Al Faqih Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii katika *Tuhfah Al Muhtaj*.

Na kwa upande wa Muwwafaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye ameelezea Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kwa kusema kua: '**Amesema Salih kua amenukuu kutoka kwa Baba yake kua, Kuna Mwanammke alikua akilalamika Kutokwa na Upepo katika Tupu yake ya Mbele,hivyo nae akamwambia kua:Chochote kile Kitakachotoka katika Tupu ya Mbele ya Mwanamme au ya Mwanammke hua kinapelekea kubatilishika kwa Udhu**.' (*Al Mugni)* Na huo pia ndio Mtizamo wa Imam Al Mardawi Al Hanbal katika *Al Insaaf.*

Hivyo ingawa huo ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na kubatilika kwa Udhu kutokana na kutokwa na kitu katika sehemu za siri za Mbele na Nyuma za Mwanammke na Mwanamme. Lakini kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi wao wanamtizamo tofauti kuhusiana na Gesi itakayotoka katika Utupu wa Mbele iwe wa Mwanammke au wa Mwanamme.

Kwani anasema Imam Al Kasani Al Hanafi kua; '**Udhu hua haubatiliki kutokana na kutoka kwa Hewe katika Tupu ya mbele ya Mtu na hii ni kwa sababu tukio hilo hutokana na Mtetemeko au Mbano, hata tukisema kua ni Upepo na hii ni kwa sababu Upepo huo hautokei kutoka katika sehemu yenye Uchafu na hivyo haubatilishi Udhu.**'*(Badai Al Sanai)*

Na akasema Imam Ad Dardir Al Maliki kua: '**Kama ikiwa kitu kisichokua cha Kawaida kitatoka nje ya mwili kwa kupitia njia Mbili tofauti na njia za kawaida**. **Kwa mfano labda kwa kupitia Mdomoni, au Mkojo ukapitia katika Njia ya Nyuma au Upepo ukapitia katika njia ya mbele hata**

katika Uchi wa Mwanammke wa Mbele, au katika tundu nyengine basi hautobatilishika Udhu wa Mtu husika.'(*Sharh Al Kabir Maa Hashiyat Al Dasuqi)*

TAYAMMAM

❖❖❖❖

Neno Tayammam limetokana na neno Yuma ambalo kwa Lugha ya Kiarabu hua linamaanisha Kutumbukizwa Ndani ya Mto, Kusafisha Uso na Mikono kwa Kutumia Vumbi la Mchanga, Kukusudia, Kua na Malengo, Kua Na Nia, Kuendelea Mbele zaidi na Jambo Husika.

Neno Yumma pia limetoa neno Yamm ambalo humaanisha Mto, Mafuriko na pia humaanisha Bahari isiokua Kubwa.

Neno Yamma ndio lililotoa neno Tayammam ambalo humaanisha hatua za kujitojarisha kwa kutumia Mchanga Uliokua Tohara, au Kwenye Udongo tohara au Sehemu kavu yenye vumbi ya Ardhi iliyokua Tohara kwa kupiga Viganja vya Mikono Juu ya Mchanga huo na kisha kupangusia viganja hivyo kwenye Mikono hadi kwenye visugudi na pia kwenye Uso kama kwamba inavyokoshwa kwa Maji.

Neno Tayammam limetajwa ndani ya Quran katika Aya zenye amrisho lenye kuainisha aina za njia Za kujitojarisha, ambazo ni kwa Kutumia Maji au Kutumia Vumbi Safi la Mchanga pale itakapokosekana Maji kama Alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ إِذَا قُمْتُمْ إِلَى ٱلصَّلاةِ فٱغْسِلُواْ وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى ٱلْمَرَافِقِ وَٱمْسَحُواْ بِرُؤُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى ٱلْكَعْبَينِ وَإِن كُنتُمْ جُنُباً فَٱطَّهَّرُواْ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىَ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ ٱلْغَائِطِ أَوْ لاَمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيداً طَيِّباً فَٱمْسَحُواْ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِّنْهُ مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَـٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

Yaaa aiyuhal ladheena aamanoo izaa qumtum ilas Salaati faghsiloo wujoohakum wa Aidiyakum ilal maraafiqi wamsahoo biru'oosikum wa arjulakum ilal ka'bayn; wa in kuntum junuban fattahharoo; wain kuntum mardhaaa aw'alaa safarin aw jaaa'a ahadum minkum minal ghaaa'iti aw laamastumu nnisaaa'a falam tajidoo maaa'an fatayammamoo sa'eedan taiyiban famsahoo biwujoohikum wa aideekum minh; ma yureedul laahu liyaj'ala 'alaikum min harajinw walaakiny yureedu liyutahhirakum wa liyutimma ni'matahoo 'alaikum la'allakum tashkuroon. *(Surat Al Maidah 5:6)*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Mtakapokusudia Kusimamisha Sala, basi kosheni nyuso zenu na mikono yenu hadi kwenye visugudi, futeni (kwa kutia maji mikono yetu) vichwa vyenu, na mkoshe miguu yenu hadi kwenye kifundo chake. Ikiwa mko katika hali ya Janaba, basi jitoharisheni. Lakini ikiwa mnaumwa au mko safarini au mkiwa mmetoka kujisaidia au lamastumu alnnisaa (mkiwa mmegusana na wanawake) na hamkupata maji yeyote, basi fanyeni Tayamam kwa kutumia mchanga ulio safi na mjipanguse kutokana nao katika mikono yenu na nyuso zenu. Allah hataki kukujaalieni ugumu katika mambo, bali anataka kukutoharisheni, na mkamilishe aliyokufanyieni juu yenu ili muwe wenye kushukuru.***

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin Imam Al Mushaqqiqn Imam Al Ghazali Al Thani Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Umar Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kuhusiana na Aya hii kua: '**Maneno yasemayo *"Idha Kuntum Al ssalati* - Mtakapojitayarisha kwa Sala" ni yenye Kiashirio kilichofichika cha Tayammam ambayo imeelezewa Mwishoni Mwa aya na hivyo Kuashiria kuaTayammam inatakiwa Kufanywa kama Yakikosekana Maji pale itakapokua Tayari Mtu anataka Kusali, na wala si Kabla ya Mda wa Sala.'***(Mafatih Al Ghayb)***

Na amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika aya nyengine kua:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقۡرَبُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنتُمۡ سُكَٰرَىٰ حَتَّىٰ تَعۡلَمُواْ مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغۡتَسِلُواْۚ وَإِن كُنتُم مَّرۡضَىٰٓ أَوۡ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوۡ جَآءَ أَحَدٞ مِّنكُم مِّنَ ٱلۡغَآئِطِ أَوۡ لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمۡ تَجِدُواْ مَآءٗ فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدٗا طَيِّبٗا فَٱمۡسَحُواْ بِوُجُوهِكُمۡ وَأَيۡدِيكُمۡۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَفُوّٗا غَفُورٗا﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo la taqraboo alssalata waantum sukara hatta taAAlamoo ma taqooloona wala junuban illa AAabiree sabeelin hatta taghtasiloo wa-in kuntum marda aw AAala safarin aw jaa ahadun minkum mina algha-iti aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban faimsahoo biwujoohikum waaydeekum inna Allaha kana AAafuwwan ghafooran. *(Surat An Nisaa 4:43).*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Msiikaribie Sala wakati mkiwa mmelewa hadi pale mtakapojua maana ya mkisemacho, wala mkiwa katika hali ya janaba isipokua pale mtakapokua safarini (bila ya kua na maji ya kutosha), hadi mtakapokosha mwili wenu wote. Na mkiwa mnaumwa, au mko safarini au mnapoenda haja au mnapo (لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi, kupangusa nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Allah ni mwingi wa kusamehe na msamehevu sana'.***

Ambapo Wanazuoni wanakubaliana kua Aya hizi zimebeba mambo saba muhimu ambayo yote yako katika hali ya kua ni peya yaani mawili mawili kama ifuatavyo:

1-Aina Mbili za Kujitoharisha Kwa Maji na Kwa Mchanga.
2-Aina mbili za Kujitoharisha kwa sehemu tu za Mwili kwa Udhu na Kwa Mwili Mzima yaani Kukoga Janaba.
3-Aina Mbili za Kujitoharisha kwa Kukosha Viungo Vya Mwili na kwa Kupangusa.
4-Aina Mbili za Vitoharisho ambavyo ni Maji na Mchanga.
5-Aina Mbili zinazompelekea Mtu kutakiwa kujitoharisha yaani Najis ndogo na Najis Kubwa.
6-Aina mbili za hali zinazomruhusu Mtu kufanya Tayamma yaani Kua Mgonjwa Au Safarini.
7-Aina mbili za Malipo ambayo ni Kua Tohara na kupata Fadhila za Allah Subhanah wa Ta'ala.

Hivyo katika Qur'an basi tumeona Amrisho la Tayammam kutoka katika aya ya 6 ya Surat Al Maidah na pia katika Surat An Nisaa aya ya 43. Na Miongoni mwa hadith basi zinazohusishwa na aya za Tayammam ni Pamoja na ifuatayo:

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ يُوسُفَ، قَالَ أَخْبَرَنَا مَالِكٌ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ الْقَاسِمِ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ عَائِشَةَ، زَوْجِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَتْ خَرَجْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فِي بَعْضِ أَسْفَارِهِ، حَتَّى إِذَا

كُنَّا بِالْبَيْدَاءِ ـ أَوْ بِذَاتِ الْجَيْشِ ـ انْقَطَعَ عِقْدٌ لِي، فَأَقَامَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَلَى الْتِمَاسِهِ، وَأَقَامَ النَّاسُ مَعَهُ، وَلَيْسُوا عَلَى مَاءٍ، فَأَتَى النَّاسُ إِلَى أَبِي بَكْرٍ الصِّدِّيقِ فَقَالُوا أَلاَ تَرَى مَا صَنَعَتْ عَائِشَةُ أَقَامَتْ بِرَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم وَالنَّاسِ، وَلَيْسُوا عَلَى مَاءٍ، وَلَيْسَ مَعَهُمْ مَاءٌ. فَجَاءَ أَبُو بَكْرٍ وَرَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم وَاضِعٌ رَأْسَهُ عَلَى فَخِذِي قَدْ نَامَ فَقَالَ حَبَسْتِ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم وَالنَّاسَ، وَلَيْسُوا عَلَى مَاءٍ، وَلَيْسَ مَعَهُمْ مَاءٌ. فَقَالَتْ عَائِشَةُ فَعَاتَبَنِي أَبُو بَكْرٍ، وَقَالَ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ يَقُولَ، وَجَعَلَ يَطْعُنُنِي بِيَدِهِ فِي خَاصِرَتِي، فَلاَ يَمْنَعُنِي مِنَ التَّحَرُّكِ إِلاَّ مَكَانُ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَلَى فَخِذِي، فَقَامَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم حِينَ أَصْبَحَ عَلَى غَيْرِ مَاءٍ، فَأَنْزَلَ اللَّهُ آيَةَ التَّيَمُّمِ فَتَيَمَّمُوا. فَقَالَ أُسَيْدُ بْنُ الْحُضَيْرِ مَا هِيَ بِأَوَّلِ بَرَكَتِكُمْ يَا آلَ أَبِي بَكْرٍ. قَالَتْ فَبَعَثْنَا الْبَعِيرَ الَّذِي كُنْتُ عَلَيْهِ، فَأَصَبْنَا الْعِقْدَ تَحْتَ

Anasema Abdillahi Ibn Yusuf kua amesema Malik kua amesema Abd Rahman Ibn Kasim kua amesema Baba yake kua amesema Aisha Radhi Allahu Anha kua: Tulitoka na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam katika Moja kati ya Safari zake tukafika Al Baida au Dhatul Jaish Na mkufu wangu uliokua Umekatika ukanidondoka na kupotea.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akabakia na baadhi ya watu kwa ajili ya kuutafuta, na ilikua hakuna Maji katika sehemu hio. Hivyo watu wakaenda kwa Abu Bakr Radhi Allahu Anhu na kumwambia: 'Hivi Jee umeona aliyoyafanya Aisha? Amemfanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kubakia katika sehemu ambayo haina Maji, na wao pia hawana Maji Hivyo Abu Bakr akaja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati akiwa amelala kwa kuweka Kichwa hake kwenye Paja langu.

Na kisha akaniambia mimi kua: 'Umemzuia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kubakia katika sehemu isiokua na Maji huku Wao wakiwa hawana hata Maji?.'

Hivyo akanigombeza na kusema yale aliyojaaliaa na Allah kuyasema na kisha akanipiga kibao kwa mkono wake. Ambapo hakuna kilichoweza kunipelekea mimi nisitikisike Isipokua kichwa cha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwenye Paja langu.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamka Alfajir huku kukiwa hakuna Maji, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha Aya ya Kutayammam, na hivyo Watu wote wakafanya Tayammam.**

Na Usaid Ibn Hudayr akasema: 'Enyi Familia ya Abu Bakr Hii sio Neema ya mwanzo Juu yenu.' Kisha Ngamia ambae niliekua nampandia Mimi akayanyanyuka na Mkufu ukaonekana chini yake*(Sahih Bukhari)*

Na katika hadith nyengine basi Imam Al Bukhari anasema kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ سِنَانٍ، قَالَ حَدَّثَنَا هُشَيْمٌ، ح قَالَ وَحَدَّثَنِي سَعِيدُ بْنُ النَّضْرِ، قَالَ أَخْبَرَنَا هُشَيْمٌ، قَالَ أَخْبَرَنَا سَيَّارٌ، قَالَ حَدَّثَنَا يَزِيدُ ـ هُوَ ابْنُ صُهَيْبٍ الْفَقِيرُ ـ قَالَ أَخْبَرَنَا جَابِرُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى " أُعْطِيتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ قَبْلِي نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ، وَجُعِلَتْ لِيَ الله عليه وسلم قَالَ الأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهُورًا، فَأَيُّمَا رَجُلٍ مِنْ أُمَّتِي أَدْرَكَتْهُ الصَّلاَةُ فَلْيُصَلِّ، وَأُحِلَّتْ لِيَ الْمَغَانِمُ وَلَمْ تَحِلَّ لأَحَدٍ قَبْلِي، وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ، وَكَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً، وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً ".

Amesema Muhammad Ibn Sinan kua amesema Hushaym, kua amesema Said Ibn Nasir kua amesema Hushayma kua amesema Sayaru kua amesema Yazidu kua amesema Suhaybah Al Faqir kua amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:
Hakika mimi nimepewa Mambo matano ambayo hakupewa Mtu yeyote kabla yangu:

1-Nimepewa Ushindi Mkubwa sana na Allah wa kuwatisha Maadui zangu kwa umbali wa masafa ya Safari ya Mwezi Mmoja.

2-Ardhi imejaalowa kua ni sehemu Tohara ya Kusalia kwangu Mimi na Ummah wangu, na Kufanyia Tayammam, hivyo Watu wa Ummah wangu wanaweza kusali popote Itakapowafikia wakati wa Sala.

3-Ngawira imehalalishwa kwangu jambo ambalo halikuwahi kuhalalishwa kwa yeyote hapo kabla.

4-Nimepewa Haki ya Kuwaombea Watu katika Siku ya Malipo.

5-Kila Mtume aliewahi kutumwa alikua akitumwa kwa ajili ya Watu waeke isipokua Mimi ambae nimetumwa kwa Watu wote.*(Sahih Bukhari)*

Na kuna hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ بُكَيْرٍ، قَالَ حَدَّثَنَا اللَّيْثُ، عَنْ جَعْفَرِ بْنِ رَبِيعَةَ، عَنِ الأَعْرَجِ، قَالَ سَمِعْتُ عُمَيْرًا، مَوْلَى ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ أَقْبَلْتُ أَنَا وَعَبْدُ اللَّهِ بْنُ يَسَارٍ، مَوْلَى مَيْمُونَةَ زَوْجِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم حَتَّى دَخَلْنَا عَلَى أَبِي جُهَيْمِ بْنِ الْحَارِثِ بْنِ الصِّمَّةِ الأَنْصَارِيِّ فَقَالَ أَبُو الْجُهَيْمِ أَقْبَلَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم مِنْ نَحْوِ بِئْرِ جَمَلٍ، فَلَقِيَهُ رَجُلٌ فَسَلَّمَ عَلَيْهِ، فَلَمْ يَرُدَّ عَلَيْهِ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم حَتَّى أَقْبَلَ عَلَى الْجِدَارِ، فَمَسَحَ بِوَجْهِهِ وَيَدَيْهِ، ثُمَّ رَدَّ عَلَيْهِ السَّلاَمَ.

Amesema Yahya Ibn Bukayr kua amesema Al Layth kua amesema Jafar Ibn Rabiah kua amesema Al Aaraj kua amesema Umayr kua tulikutana mimi na Abd Allahi Ibn Yasir aliekua Mtumwa wa Maymunah Mke wa *Rasul Allah Salllahu Alayi wa Salam* hadi tukaingia kwa Abi Juhaymi Ibn Harith Ibn Simati Al Ansari Akasema Abu Juhaymi: 'Nilikutana na *Rasul Allah*

Salallahu Alayhi wa Salam **katika Upande wa Bir Jamal. Na kuna Mtu akakutana nae na kumsalimia, lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakujibu Salam, hadi pale alipofika kwenye Ukuta wa Nyumba ya Udongo, na kisha akajipangusia Uso wake na mikono yake kutokana na Vumbi lake (Kutayammam) na kisha ndio akarudisha Salam hio.''***(Sahih Bukhari)***

Na kuna hadith isemayo kua

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ سَلاَمٍ، قَالَ أَخْبَرَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، عَنِ الأَعْمَشِ، عَنْ شَقِيقٍ، قَالَ كُنْتُ جَالِسًا مَعَ عَبْدِ اللَّهِ وَأَبِي مُوسَى الأَشْعَرِيِّ فَقَالَ لَهُ أَبُو مُوسَى لَوْ أَنَّ رَجُلاً أَجْنَبَ، فَلَمْ يَجِدِ الْمَاءَ شَهْرًا، أَمَا كَانَ يَتَيَمَّمُ فَقَالَ {فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا}وَيُصَلِّي فَكَيْفَ تَصْنَعُونَ بِهَذِهِ الآيَةِ فِي سُورَةِ الْمَائِدَةِ عَبْدُ اللَّهِ لَوْ رُخِّصَ لَهُمْ فِي هَذَا لأَوْشَكُوا إِذَا بَرَدَ عَلَيْهِمُ الْمَاءُ أَنْ يَتَيَمَّمُوا الصَّعِيدَ. قُلْتُ وَإِنَّمَا كَرِهْتُمْ هَذَا لِذَا قَالَ نَعَمْ. فَقَالَ أَبُو مُوسَى أَلَمْ تَسْمَعْ قَوْلَ عَمَّارٍ لِعُمَرَ بَعَثَنِي رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فِي حَاجَةٍ فَأَجْنَبْتُ، فَلَمْ أَجِدِ الْمَاءَ، فَتَمَرَّغْتُ فِي الصَّعِيدِ كَمَا تَمَرَّغُ الدَّابَّةُ، فَذَكَرْتُ ذَلِكَ لِلنَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَقَالَ " إِنَّمَا كَانَ يَكْفِيكَ أَنْ تَصْنَعَ هَكَذَا ". فَضَرَبَ بِكَفِّهِ ضَرْبَةً عَلَى الأَرْضِ ثُمَّ نَفَضَهَا، ثُمَّ مَسَحَ بِهَا ظَهْرَ كَفِّهِ بِشِمَالِهِ، أَوْ ظَهْرَ شِمَالِهِ بِكَفِّهِ، ثُمَّ مَسَحَ بِهِمَا وَجْهَهُ فَقَالَ عَبْدُ اللَّهِ أَفَلَمْ تَرَ عُمَرَ لَمْ يَقْنَعْ بِقَوْلِ عَمَّارٍ وَزَادَ يَعْلَى عَنِ الأَعْمَشِ عَنْ شَقِيقٍ كُنْتُ مَعَ عَبْدِ اللَّهِ وَأَبِي مُوسَى فَقَالَ أَبُو مُوسَى أَلَمْ تَسْمَعْ قَوْلَ عَمَّارٍ لِعُمَرَ إِنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم بَعَثَنِي أَنَا وَأَنْتَ فَأَجْنَبْتُ فَتَمَعَّكْتُ بِالصَّعِيدِ، فَأَتَيْنَا رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَأَخْبَرْنَاهُ فَقَالَ " إِنَّمَا كَانَ يَكْفِيكَ هَكَذَا ". وَمَسَحَ وَجْهَهُ وَكَفَّيْهِ وَاحِدَةً

Amesema Muhammad Ibn Salami kua amesema Abu Muawwiyah kua amesema Al Amash kua: Amesema Shaqiq kua: 'Mimi nilikua nimekaa na Abd Allah na Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhum*, ambapo Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu*akamuuliza Abd Allah *Radhi Allahu Anhu*: 'Hivi kama kwa Mfano ikiwa Mtu amekua na Janaba na kisha akawa hajapata Maji kwa Mda wa Mwezi Mzima, Jee anaweza kufanya Tayammam na kisha Akasali?''

Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'La!'

Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama ni hivyo basi Jee unasemaje wewe kuhusiana na hii aya ya Surat Al Maidah iliyosema:

{فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا}

FFalam tajidoo maaa'an fatayammamoo sa'eedan taiyiban - Na Kama Hamkupata Maji Basi Fanyeni Tayammam kwa Mchanga Uliosafi na Mzuri*(Surat Al Maidah 5:6)*

Ambapo Abd Allah akajibu kwa kusema kua: 'Kama tukiruhusu hivyo basi Watu watafanya Tayammam kutokana na Baridi hata kama Maji yapo.'

Hivyo Imam Al Amash akamwambia Imam Al Shaqiq Anaeelezea Hadith hii kwa kusema kua: 'Ndio Maana wewe hupendi kufanya Tayammam, Jee ni kwa sababu ya hii?'

Imam Shaqiq akasema: 'Naam!' kisha akaendelea kusema kua: 'Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Hivi Jee hujasikia wewe Kauli ya Ammar Ibn Yasir aliyomwambia Umar Ibn Al Khattab Radhi Allahu Anhum? Kwa kusema: Mimi nilitumwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kutekeleza Jambo fulani, na nikawa na Janaba.'

'Na hivyo nikashindwa kupata Maji, Hivyo nikajigaragaza kwenye mchanga, Kama wanavyofanya Wanyama. Na kisha niliporudi nikamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya Tukio hilo, ambapo nae akasema: 'Kama ungefanya Hivi tu basi ingekutosheleza.' Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akaipiga kidogo mikono yake, juu ya mchanga mara moja na kisha akaipuliza na kisha akaupitisha mkono wake wa kushoto juu ya mkono wa kulia na mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto na kisha akapangusia mikono yake hio kwenye uso wake.''

Imam Al Shaqiq akaendelea kusema kua Ambapo Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhum* kwa kusema: 'Hivi jee wewe hujui kua Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhum* hakutosheka na Kauli ya Ammar *Radhi Allahu Anhu?'*

Shaqiq amesema kua: 'Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Hivi Jee hujasikia wewe Kauli ya Ammar Ibn Yasir aliyomwambia Umar Ibn Al Khattab Radhi Allahu Anhum? Kwa kusema: Mimi nilitumwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kutekeleza Jambo fulani, na nikawa na Janaba.'

'Na hivyo nikashindwa kupata Maji, Hivyo nikajigaragaza kwenye mchanga, Kama wanavyofanya Wanyama. Na kisha niliporudi nikamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya Tukio hilo, ambapo nae akasema: 'Kama ungefanya Hivi tu basi ingekutosheleza' Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akaipiga kidogo mikono yake, juu ya mchanga mara moja na kisha akaipuliza na kisha akaupitisha mkono wake wa kushoto juu ya mkono wa kulia na mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto na kisha akapangusia mikono yake hio kwenye uso wake.''*(Sahih Bukhari)***

Na pia kuna hadith isemayo:

حَدَّثَنَا مُسَدَّدٌ، قَالَ حَدَّثَنِي يَحْيَى بْنُ سَعِيدٍ، قَالَ حَدَّثَنَا عَوْفٌ، قَالَ حَدَّثَنَا أَبُو رَجَاءٍ، عَنْ عِمْرَانَ، قَالَ كُنَّا فِي سَفَرٍ مَعَ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم وَإِنَّا أَسْرَيْنَا، حَتَّى كُنَّا فِي آخِرِ اللَّيْلِ، وَقَعْنَا وَقْعَةً وَلاَ وَقْعَةَ أَحْلَى عِنْدَ الْمُسَافِرِ مِنْهَا، فَمَا أَيْقَظَنَا إِلاَّ حَرُّ الشَّمْسِ، وَكَانَ أَوَّلَ مَنِ اسْتَيْقَظَ فُلاَنٌ ثُمَّ فُلاَنٌ ثُمَّ فُلاَنٌ ثُمَّ فُلاَنٌ . يُسَمِّيهِمْ أَبُو رَجَاءٍ فَنَسِيَ عَوْفٌ . ثُمَّ عُمَرُ بْنُ الْخَطَّابِ الرَّابِعُ، وَكَانَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم إِذَا نَامَ

لَمْ يُوقَظْ حَتَّى يَكُونَ هُوَ يَسْتَيْقِظُ، لأَنَّا لاَ نَدْرِي مَا يَحْدُثُ لَهُ فِي نَوْمِهِ، فَلَمَّا اسْتَيْقَظَ عُمَرُ، وَرَأَى مَا أَصَابَ النَّاسَ، وَكَانَ رَجُلاً جَلِيدًا، فَكَبَّرَ وَرَفَعَ صَوْتَهُ بِالتَّكْبِيرِ، فَمَا زَالَ يُكَبِّرُ وَيَرْفَعُ صَوْتَهُ بِالتَّكْبِيرِ حَتَّى اسْتَيْقَظَ لِصَوْتِهِ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم فَلَمَّا اسْتَيْقَظَ شَكَوْا إِلَيْهِ الَّذِي أَصَابَهُمْ قَالَ " لاَ ضَيْرَ ـ أَوْ لاَ يَضِيرُ ـ ارْتَحِلُوا ". فَارْتَحَلَ فَسَارَ غَيْرَ بَعِيدٍ ثُمَّ نَزَلَ، فَدَعَا بِالْوَضُوءِ، فَتَوَضَّأَ وَنُودِيَ بِالصَّلاَةِ فَصَلَّى بِالنَّاسِ، فَلَمَّا انْفَتَلَ مِنْ صَلاَتِهِ إِذَا هُوَ بِرَجُلٍ مُعْتَزِلٍ لَمْ يُصَلِّ مَعَ الْقَوْمِ قَالَ " مَا مَنَعَكَ يَا فُلاَنُ أَنْ تُصَلِّيَ مَعَ الْقَوْمِ ". قَالَ أَصَابَتْنِي جَنَابَةٌ وَلاَ مَاءَ. قَالَ " عَلَيْكَ بِالصَّعِيدِ، فَإِنَّهُ يَكْفِيكَ ". ثُمَّ سَارَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم فَاشْتَكَى إِلَيْهِ النَّاسُ مِنَ الْعَطَشِ فَنَزَلَ، فَدَعَا فُلاَنًا ـ كَانَ يُسَمِّيهِ أَبُو رَجَاءٍ نَسِيَهُ عَوْفٌ ـ وَدَعَا عَلِيًّا فَقَالَ " اذْهَبَا فَابْتَغِيَا الْمَاءَ ". فَانْطَلَقَا فَتَلَقَّيَا امْرَأَةً بَيْنَ مَزَادَتَيْنِ ـ أَوْ سَطِيحَتَيْنِ ـ مِنْ مَاءٍ عَلَى بَعِيرٍ لَهَا، فَقَالاَ لَهَا أَيْنَ الْمَاءُ قَالَتْ عَهْدِي بِالْمَاءِ أَمْسِ هَذِهِ السَّاعَةَ، وَنَفَرُنَا خُلُوفًا. قَالاَ لَهَا انْطَلِقِي إِذًا. قَالَتْ إِلَى أَيْنَ قَالاَ إِلَى رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم. قَالَتِ الَّذِي يُقَالُ لَهُ الصَّابِئُ قَالاَ هُوَ الَّذِي تَعْنِينَ فَانْطَلِقِي. فَجَاءَا بِهَا إِلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم وَحَدَّثَاهُ الْحَدِيثَ قَالَ فَاسْتَنْزَلُوهَا عَنْ بَعِيرِهَا وَدَعَا النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم بِإِنَاءٍ، فَفَرَّغَ فِيهِ مِنْ أَفْوَاهِ الْمَزَادَتَيْنِ ـ أَوِ السَّطِيحَتَيْنِ ـ وَأَوْكَأَ أَفْوَاهَهُمَا، وَأَطْلَقَ الْعَزَالِيَ، وَنُودِيَ فِي النَّاسِ اسْقُوا وَاسْتَقُوا. فَسَقَى مَنْ شَاءَ، وَاسْتَقَى مَنْ شَاءَ، وَكَانَ آخِرَ ذَاكَ أَنْ أَعْطَى الَّذِي أَصَابَتْهُ الْجَنَابَةُ إِنَاءً مِنْ مَاءٍ قَالَ " اذْهَبْ، فَأَفْرِغْهُ عَلَيْكَ ". وَهْيَ قَائِمَةٌ تَنْظُرُ إِلَى مَا يُفْعَلُ بِمَائِهَا، وَايْمُ اللَّهِ لَقَدْ أُقْلِعَ عَنْهَا، وَإِنَّهُ لَيُخَيَّلُ إِلَيْنَا أَنَّهَا أَشَدُّ مِلأَةً مِنْهَا حِينَ ابْتَدَأَ فِيهَا، فَقَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " اجْمَعُوا لَهَا ". فَجَمَعُوا لَهَا مِنْ بَيْنِ عَجْوَةٍ وَدَقِيقَةٍ وَسَوِيقَةٍ، حَتَّى جَمَعُوا لَهَا طَعَامًا، فَجَعَلُوهَا فِي ثَوْبٍ، وَحَمَلُوهَا عَلَى بَعِيرِهَا، وَوَضَعُوا الثَّوْبَ بَيْنَ يَدَيْهَا قَالَ لَهَا " تَعْلَمِينَ مَا رَزِئْنَا مِنْ مَائِكِ شَيْئًا، وَلَكِنَّ اللَّهَ هُوَ الَّذِي أَسْقَانَا ". فَأَتَتْ أَهْلَهَا، وَقَدِ احْتَبَسَتْ عَنْهُمْ قَالُوا مَا حَبَسَكِ يَا فُلاَنَةُ قَالَتِ الْعَجَبُ، لَقِيَنِي رَجُلاَنِ فَذَهَبَا بِي إِلَى هَذَا الَّذِي يُقَالُ لَهُ الصَّابِئُ، فَفَعَلَ كَذَا وَكَذَا، فَوَاللَّهِ إِنَّهُ لأَسْحَرُ النَّاسِ مِنْ بَيْنِ هَذِهِ وَهَذِهِ. وَقَالَتْ بِإِصْبَعَيْهَا الْوُسْطَى وَالسَّبَّابَةِ، فَرَفَعَتْهُمَا إِلَى السَّمَاءِ ـ تَعْنِي السَّمَاءَ وَالأَرْضَ ـ أَوْ إِنَّهُ لَرَسُولُ اللَّهِ حَقًّا، فَكَانَ الْمُسْلِمُونَ بَعْدَ ذَلِكَ يُغِيرُونَ عَلَى مَنْ حَوْلَهَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ، وَلاَ يُصِيبُونَ الصِّرْمَ الَّذِي هِيَ مِنْهُ، فَقَالَتْ يَوْمًا لِقَوْمِهَا مَا أُرَى أَنَّ هَؤُلاَءِ الْقَوْمَ يَدَعُونَكُمْ عَمْدًا، فَهَلْ لَكُمْ فِي الإِسْلاَمِ فَأَطَاعُوهَا فَدَخَلُوا فِي الإِسْلاَمِ.

AL MUSTAKSHIF ABU MANAL DANAH

Musaddad amesema kua, amesema Yahya Ibn Said, kua Awf amesema kua: amesema Abu Raja kua amesema Imran; 'Sisi Tulikuwa safarini pamoja na *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*, na hakuna tukasafiri mpaka mwisho wa sehemu ya Usiku, na hakuna Usingizi Mtamu kwa Msafiri kama usingizi wa mwishoni mwa sehemu ya Usiku. Hivyo tulipolala basi hakuna kilichotuamsha isipokuwa joto la Jua, na wa kwanza kuamka alikuwa hivi na fulani, kisha fulani. Kisha fulani fulani - Abu Raja' aliwataja majina yao, lakini Awf aliyasahau - basi Umar Ibn Al-Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambae alikuwa ni wa nne kuamka.

Na *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*, alikua anapolala, ilikuwa haamshwi mpaka azindukane mwenyewe, kwa sababu hatujui yanayomtokea usingizini huenda ikawa anashushiwa Wahyi. Hivyo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alipozinduka na kuona yaliyowafika watu, na yeye ni mtu mwenye msimamo, basi akasema *Allahu Akbar* na kisha akapaza sauti yake kwa Takbir, na akaendelea kusema *Allahu Akbar* na kupaza sauti kwa Takbir. Hadi *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*, akaamka kwa sauti hio ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*

***Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*, alipozindukana, Masahaba Radhi Allau Anhum wakawmlalamikia kwa kile kilichotokea na *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*, akasema: "Hakuna madhara - au haidhuru – Tuondoke na kuendelea na Safari."**

Hivyo Msafara ukoandoka kutoka katika sehemu hio na baada ya kufikika masafa mafupi kidogo basi *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*, akasonga mbele na akasafiri sio mbali, kisha akateremka, akaitisha wudhuu, akatawadha, na ukatolewa wito wa kuswali, hivyo akawaongoza watu katika swala. Alipomaliza sala yake, alimuona mtu ambaye alikuwa aakasimamisha Msafara na kisha akaomba Maji ya Kutawadha, akatia Udhu na kisha ikaadhiniwa Adhana na *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*, akasalisha na baada ya kumaliza kusali akamuona Mtu akiwa amekaa pembeni peke yake bila y akua ni mwenye kusali Pamoja na wenzake.

Hivyo *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Mtu huyo: 'Ewe Fulani, Hivi ni kitu gani kilichokuzuia wewe kutosali Pamoja na Sisi?' ambapo Mtu huyo akasema: 'Ya Rasul Allah Hakika mimi nimejikuta kua nna Janaba na hakuna Maji'. *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Fanya Tayammam kwakutumia Udongo Msafi naitakutosheleza.'

Na kisha *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akaendelea na Safari na watu wakaanza kumlalamikia kuhusiana na Kiu. Na hivyo *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akasimamisha msafara na kushuka kutoka kwenye Ngamia wak na akamwia mmoja kati ya Watu (ambapo Awf amesema kua Abu Raja' amemtaja jina lake lakini yeye amemsahau) na Ali Ibn Abialib *Radhi Allahu Anhu* na kuwaamrisha kutafuta Maji, na wakatoka kutafuta Maji na wakamkuta Mwanammke akiwa amepanda Ngamia wake huku akiwa amekaa baina ya Mabuyu mawili ya Maji.

Hivyo wakamuuliza: 'Jee wapi tunaweza kupata Maji?' yule Mwanammke akajibu kua: 'Mimi Jana ndio nilikua kwenye sehemu yenye Maji, na watu wangu wanafata nyuma baada yangu' hivyo nao wakamuomba kua waende awafuate, na akawauliza: 'Nkufuateni wapi?' nao wakasema: 'Kwa *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam*' Mwanammke huyo akasema: 'Mnamaanisha yule Mtu anaeitwa Sabbi(Mwenye Dini Mpya)?' Nao wakasema : 'Naam. Hivyo twende kwake pamoja'.

Hivyo wakaenda nae hadi kwa *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* na wakamuelezea, na kisha *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akaamrisha kwa kusema: 'Msaidieni kushuka kutoka kwenye Ngamia wake.' Na hivyo Mwanammke huyo akasaidiwa kuteremka kwenye Ngamia wake

na kisha *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akaomba aletewe Mtungi na kisha akafufungua midomo ya vibuyu vya Maji hayo, na akamiminia Maji hayo ndani ya Mtungi.

Na kisha akafunga mdomo mkubwa wa Vibuyu na kufungua Mdomo mdogo wa Vibuyu na akawaita watu waje kunywa Maji na wanyweshe Wanyama wao pia. Hivyo Watu wakawanywesha maji Wanyama wao na wao pia wakanywa na kuondoa Kiu zao, na kuwapa Maji watu wengine na wa mwisho *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akampa Maji yule Mtu aliekua na Janaba na kumwambia ajimwagie Mwilini mwake, huku yule Mwanammke akiwa amesimama akiangalia namna yanavyofanywa Maji yake.

Wa Allahi! Alipokabidhiwa Vibuyu vya Maji yake na kuangalia ndani yake akaona kua Maji yake yamebakia kama yalivyokua hapo kabla, na kisha *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akaamrisha kukusanywe baadhi ya vitu kwa ajili yake hivyo Tende, Unga, na Sawiq zikakusanywa ambavyo ni vyenye kujumuisha chakula cha kutosha vikafungwa kwenye Bahasha ya Kitambaa, na kisha akasaidiwa kupanda juu ya Ngamia wake na akapewa Bahasha yake ya Vyakula na kuwekewa mbele yake, na kisha *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia: 'Hakika sisi hatukuchukua Maji yako, bali *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametupa Sisi Maji kutokana nawe.'

Hivyo akarudi kwenye huku akiwa amechelewa na na watu wake wakamuuliza kwa kusema: 'Ewe Fulani mbona umechelewa ilikuaje?' ambapo nae akasema kua: 'Kuna Jambo geni sana nimeliona limenitokezea, kuna watu waili nilikutana nao njiani na wakanichukua hadi kwa Mtu ambae ni Sabina wakafanya kadhaa wa kadhaa. Wa Allahi yule Mtu hawezi kua isipokua ni Mchawi mkubwa sana baina ya haya (huku akionesha baina ya kidole chake cha shahada na kidole chake cha kati akivinyoosha na kuvielekeza juu kuashiria baina ya Mbingu na Ardhi) au ni Rasul Allahi'

Baada ya hapo Waislamu wakavamia Vijiji vya Mapagani kuzunguka maeneo anaoishi lakini hawakukigusa Kijiji chake. Siku moja akawaambia Watu wake kua: 'Hakika mimi nnafikiria kua hawa watu wamekuachieni kwa makusudi, hivyo jee hamfikirii nyiny kujiunga na Uislam?'

Hivyo watuwake hao wote wakakubaliana nae na wakingia katika Uislam. Akasema Abu Abda Allah kua: 'Neno Sabaa maana yake hua ni mtu alieacha Dini yake na kufuata Dini Mpya'. Na Abu Aliyyah amesema kua: 'Sabbi ni kundi la watu wa Ahl al Kitab ambao walikua wakisoma Tawrat' *(Sahih Bukhari.)*

Na pia kuna hadith isemayo:

حَدَّثَنَا آدَمُ، قَالَ حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، حَدَّثَنَا الْحَكَمُ، عَنْ ذَرٍّ، عَنْ سَعِيدِ بْنِ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبْزَى، عَنْ أَبِيهِ، قَالَ جَاءَ رَجُلٌ إِلَى عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ فَقَالَ إِنِّي أَجْنَبْتُ فَلَمْ أُصِبِ الْمَاءَ. فَقَالَ عَمَّارُ بْنُ يَاسِرٍ لِعُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ أَمَا تَذْكُرُ أَنَّا كُنَّا فِي سَفَرٍ أَنَا وَأَنْتَ فَأَمَّا أَنْتَ فَلَمْ تُصَلِّ، وَأَمَّا أَنَا فَتَمَعَّكْتُ فَصَلَّيْتُ، " إِنَّمَا كَانَ يَكْفِيكَ هَكَذَا ". فَذَكَرْتُ لِلنَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَقَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم فَضَرَبَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم بِكَفَّيْهِ الأَرْضَ، وَنَفَخَ فِيهِمَا ثُمَّ مَسَحَ بِهِمَا وَجْهَهُ وَكَفَّيْهِ.

Amesema Adam kua amesema Shu' bah kua amesema Al Hakamu kua maesema Dhari kua amesema Said Ibn Abd Rahman Ibn Abza kua: 'Alikuja Mtu kwa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* na kusema kua: 'Baba yangu imemsibu Janaba na hakuna Maji.'

Hivyo akasema Amaar Ibn Yasir *Radhi Allah Anhu* kumwambia Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Jee unakumbuka wakati mimi na wewe tulipokua Safarini, na wewe ukawa hukusali na mimi nikagaragara Mchangani, Na kisha niliporudi nikamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya Tukio hilo, ambapo nae akasema: 'Kama ungefanya Hivi tu basi ingekutosheleza' Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akaipiga kidogo mikono yake, juu ya mchanga mara moja na kisha akaipuliza na kisha akapangusia mikono yake hio kwenye uso wake na kwenye mikono yake.'' *'(Sahih Bukhari)*

Hivyo baada ya kuona mifano ya hadith zenye kuonesha Amrisho la Kufanya Tayammam na pia sababu za Kushushwa aya za Tayammam. Ambapo pia tunaona kua kwa upande wa Wanazuoni wa Tarikh basi wao wanasema kua: '**Tayammam kwa mara ya kwanza ilianza kutumika mnamo mwaka wa 6 Al Hijra Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipotoka na Jeshi lake kuelekea kwenye Vita dhidi ya Watu wa Banu Mustalik, na hivyo wakapiga Kambi Njiani ulipoingia wakati wa Usiku na Kulala. Hivyo walipoamka kwa ajili ya Sala ha Asubuhi ikawa hakuna Maji, na wao wenyewe Wakashindwa kupata Maji hata baada ya kufanya Jitihada, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha Aya ya Tayammam ya Surat Al Maidah isemayo.**

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ إِذَا قُمْتُمْ إِلَى ٱلصَّلاةِ فٱغْسِلُواْ وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى ٱلْمَرَافِقِ وَٱمْسَحُواْ بِرُؤُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى ٱلْكَعْبَينِ وَإِن كُنتُمْ جُنُباً فَٱطَّهَّرُواْ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ ٱلْغَائِطِ أَوْ لاَمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيداً طَيِّباً فَٱمْسَحُواْ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِّنْهُ مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَـٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

Yaaa aiyuhal ladheena aamanoo izaa qumtum ilas Salaati faghsiloo wujoohakum wa Aidiyakum ilal maraafiqi wamsahoo biru'oosikum wa arjulakum ilal ka'bayn; wa in kuntum junuban fattahharoo; wain kuntum mardhaaa aw'alaa safarin aw jaaa'a ahadum minkum minal ghaaa'iti aw laamastumu nnisaaa'a falam tajidoo maaa'an fatayammamoo sa'eedan taiyiban famsahoo biwujoohikum wa aideekum minhu; ma yureedul laahu liyaj'ala 'alaikum min harajinw walaakiny yureedu liyutahhirakum wa liyutimma ni'matahoo 'alaikum la'allakum tashkuroon. *(Surat An Maidah 5:6)*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Mtakapokusudia Kusimamisha Sala, basi kosheni nyuso zenu na mikono yenu hadi kwenye visugudi, futeni (kwa kutia maji mikono yetu) vichwa vyenu, na mkoshe miguu yenu hadi kwenye kifundo chake. Ikiwa mko katika hali ya Janaba, basi jitoharisheni. Lakini ikiwa mnaumwa au mko safarini au mkiwa mmetoka kujisaidia au lamastumu alnnisaa (mkiwa mmegusana na wanawake) na hamkupata maji yeyote, basi fanyeni Tayamam kwa kutumia mchanga ulio safi na mjipanguse kutokana nao katika mikono yenu na nyuso zenu. Allah hataki kukujaalieni ugumu katika mambo, bali anataka kukutoharisheni, na mkamilishealiyokufanyieni juu yenu ili muwe wenye kushukuru.***'

Na ingawa tumeona hadith zisemazo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alionesha namna ya Kuia Udhu kwa Mchanga au kwa Tayammum kwa Kutumia Hatua Moja tu ya Kupiga Mikono kwenye

Mchanga Safi na kisha Kupuliza viganja vyake na kujipaka Juu ya mkono wa Kulia na Kushoto na Uso mara moja tu, ambao ndio njia ya Mtizamo wa Kutayamam kunakotumiwa na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Malik.

Lakini hata hivyo pia kuna Hadith zisemazo kua:

حدثنا محمد بن مخلد وإسماعيل بن علي وعبد الباقي بن قانع، قالوا: حدثنا إبراهيم بن إسحاق الحربي، حدثنا عثمان بن أحمد الأنماطي، حدثنا حرمي بن عمارة، عن عزرة بن ثابت، عن أبي الزبير عن جابر عن النبي صلى الله عليه وسلم، قال التيمم ضربة للوجه، وضربة للذراعين إلى المرفقين

Amesema Muhammad Ibn Makhlad kua Ismail Ibn Ali na Abd Al BaqiIbn Qani kua wamesema kua: ‘Amesema Ibrahim Ibn Is-haq Al Harbi kua Usman Ibn Ahmad Al Anmati amesema kua: Harmi Ibn Umarah ametuambia kua amesema Azrah Ibn Thabit kua amesema Al Zubayr kua amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua: ‘Tayammam hua ni Pigo kwa ajili ya Uso na pigo kwa Ajili ya Mikono Miwili hadi kwenye Visugudi.’*(Sunnan Imam Ad Daraqutni)*

Na pia Hadith hii imenukuliwa kupitia katika mnyororo wa njia nyengine kama inavyothibitishwa na maneno yafuatayo kua: ‘**Amesema Ali Ibn Hamshadh na Abu Bakr Ibn Baluyah kua maesema Ibrahim Ibn Is-haq kua amesema Uthman Ibn Muhammad Al Anmati Kua amesema Harmi Ibn Umarah kua amesema Azra Ibn Thabit kua amesema Abu Al Zubayr kua amesema Jabir Ibn Abd *Allah Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua : Tayammam ni Mapigo Mawili, Pigo moja ni kwa ajili ya Uso, na Pigo la Pili ni kwa ajili ya Mikono hadi kwenye visugudi.**’ *(Sunnan Al Kubra Imam Al Bayhaqi, Mustadrak Al Sahihayn Al Hakim, Imam Al Hakim)*

Ambapo kuhusiana na Hadith hizi basi amesema Imam Al Hakim mwenyewe kua ni **Hadith Sahih na pia Imam Adh Dhahabi ameungana nae Mkono juu ya Usahih wa Hadith hizi.** Na kwa Upande wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi yeye amesema kua ni **Hasan Hadith.**

Na bila ya shaka akasema Imam Badr Al Ayni akasema kua: **‘Kwa asiekubaliana na Usahih wa Hadith hizi baada ya vithibitisho vya Usahih wake kutoka kwa Imam Al Hakim na Imam Shams Ad Din Adh Dhahabi, basi haina haja kutiliwa maanani hoja zake’***(Nukhab Al Afkar)*

Naam..hivyo Hadith tulizoziangalia leo ambazo ni hadith mbili kwa moja zenye kusema kua Tayammam ni Mapigo Mawili ya Viganja vya Mikono kwenye mchana ambalo la kwanza ni kwa Uso na kisha pigo la pili ni kwa Mikono, Basi Ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Abu Hanifa, pia kuna Mtizamo huu kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik lakini hauna nguvu kuhusiana na Tayammam ambao umezungumziwa na Imam Maalik mwenyewe katika Muwatta Imam Malka ambao amesema ndani yake kua: ‘**Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua akifanya Tayammam kwa njia ya kupiga mapigo mawili, moja kwa ajili ya Uso na la pili kwa ajili ya Mikono’**

Na pia amesema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua:

وعن عمار بن ياسر قال: كنت فى القوم حين نزلت الرخصة فأمرنا فضربنا واحدة للوجه ثم ضربة أخرى لليدين إلى المرفقين، أخرجه البزار بإسناد حسن

Amesema Ammar Ibn Yasir kua: 'Mimi nilikua ni miongoni wa Watu waliokuwepo wakati Liliposhuka amrisho la Tayammam, na Hivyo Tukapewa Maelezo na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, kua Pigo Moja ni kwa ajili ya Uso na Pigo la pili ni kwa ajili ya Mikono hadi kwenye visugudi.' Na Imam Al Bazzar amaeinukuu hadith hii kupitia kwennye Sanad Nzuri sana.'*(Al Dirayah).*

Hivyo huu Mtizamo wa Mapigo mawili ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Abu Hanifa na kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik na Hanbal basi Tayammam ni pigo moja tu la viganja kwenye Mchanga.

Na mbali ya Hadith hizi za Mapigo mawili lakini pia kuna hadithi nyengine kadhaa ambazo ziko katika hali ya kua na sifa ya Marfuu kutoka kwa Aisha, Abd Allah Ibn Umar, Abu Ummamah, Al Asla, Abu Juhaym, Abd Allah Ibn Awfana Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhum* zinazozungumzia kuunga mkono hoja ya mtizamo wa kua Tayammam ni mapigo mawili kama ilivyosemwa katika Amani Al Ahbar.

Na ipa kuna hadith isemayo kua:

حدثنا محمد بن أحمد بن أبي خلف ومحمد بن يحيى النيسابوري في آخرين قالوا: أخبرنا يعقوب أخبرنا أبي عن صالح عن ابن شهاب حدثني عبيد الله بن عبد الله عن ابن عباس عن عمار بن ياسر رضي الله عنهم:) أن رسول الله صلى الله عليه وسلم عرس بأولات الجيش ومعه عائشة رضي الله فحبس الناس ابتغاء عقدها ذلك حتى أضاء الفجر وليس :فانقطع عقد لها من جزع ظفار عنها، حبستِ الناس وليس معهم ماء، فأنزل الله :فتغيظ عليها أبو بكر رضي الله عنه وقال مع الناس ماء، تعالى ذكره على رسوله صلى الله عليه وسلم رخصة التطهر بالصعيد الطيب، فقام المسلمون مع رسول الله صلى الله عليه وسلم، فضربوا بأيديهم إلى الأرض، ثم رفعوا أيديهم ولم يقبضوا من التراب شيئاً، فمسحوا بها وجوههم وأيديهم إلى المناكب ومن بطون أيديهم إلى الآباط

Amesema Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Khalaf na Muhammad Ibn Yahya al-Nishapuri, na wengineo wamesema kua amesema Yaqub kua amesema Baba yangu kutoka kwa Salih kua amesema Ibn Shihab, kua amesema Ubayd Allah Ibn Abdullah kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua amesema Ammar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* kua:

***Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam* alienda Harusini Pamoja na Wanawake wa Kijeshi akiwa Pamoja Nae Aaisha *Radi Allahu Anha,* na hivyo Mkufu wake wenye Lakti ya Dhofar ukakatika na kumuanguka na hivyo akawazuia watu wasiendelee na Msafara ili wautafute Mkufu huo hadi Alfajiri ikaingia na ilikua hakuna Maji, na wala hakuna mwenye Maji miongoni mwa Waislam. Hivyo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akamkasirikia Aisha *Radhi Allahu Anha* na kumwambia: 'Umewazuia watu huku wakiwa hawana hata Maji Pamoja nao.'**

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha aya ya Tayammam kumruhusu kujitoharisha kwa Mchanga uliokua Safi na Tohara, hivyo Waisla wakasimama Pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Salam na wakapiga Mchangani kwa mikono yao Na kisha wakanyanyua Mikono yao bila kua na Mchanga kisha Wakajipangusia Nyusoni mwao hadi shingoni na Mikononi hadi Kwapani.'*(Sunnan Abu Daud)*

Hivyo anasema Mujaddid Ad Din Imam Shihab Ad Din Abu Fadhl Ahmad Ibn Nur Ad Din Ali Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ya kumwambia Sahaba yake Ammar Ibn Yassir *Radhi Allahu* Anhu kua Kupangusia Uso na Mikono tu kunakutosheleza Yanamaanisha kua Viungo viwili hivyo ni Wajibu na hua vinatosheleza katika Kutayamam. Kwani Hadith zote zilizonukuliwa kuhusiana na Tayammam si Hadith Sahih isipokua Hadith ya Abu Juhaym na ya Ammar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhum.***

Ambapo Udhaifu wa Hadith nyenginezo ni wenye kutokana na kutokua na uhakika wa kua zimetoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ama la, hivyo Jibu sahih itakua hazikutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Ambapo kuhusiana na Hadith za Abu Juhaym basi kuna Hadith ambayo imesema kua kupangusa Mikono hua ni kuanzia kwenye ncha za vidole hadi kwenye Visugudi na kuna Hadith isemayo hadi kwenye Kwapa.

Ama kuhusiana na Hadith inayosema kua hadi kwenye Visugudi basi ina maelezo yake, na kuhusiana na Hadith ya hadi kwapani basi Imam Al Shafii na wengine wamesema kua: 'Kama ikitokea hivyo kua ndio amrisho la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Kila Tayammam aliyoifanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* itakua Sahih baada ya Kuibatilisha ile iliyotangulia.'

Hivyo kama ikiwa haikutokana na amrisho lake, basi Ushahidi utakua ni katika lile ambalo aliloliamrisha.

Hivyo kinachoupa Nguvu uthibitisho wa Hadith za kupangusa Uso na Mikono Ni kua Ammar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* alikua akitoa Fatwa kuhusiana nazo hata baada ya kutokuwepo kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na alienukuu Hadith hua ni mwenye kujua zaidi juu ya Hadith husika kuliko Mtu yeyote yule,hususan tunapowazungumzia Masahaba wenye kua na ari juu ya kila kitu.'*(Fat-h al Barr)*

Hivyo maneno haya ya Imam Ibn Hajar Al Asqallani yanatudhihirishia kua Tayammam hua ni Kupangusa Mikononi na Usoni tu tena bila kufikisha kwapani.

Ambapo kuhusiana na Idadi ya mapigo basi anasema Muwwafaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Hanbali kua: '**Hakuna tofauti baina ya Madhhab kuhusiana na Tayammam kua inatosheleza kwa kutumia Pigo moja au mawili Kwani kama Mtu akitumia Pigo Moja, au Mawili au zaidi ya Mawili basi hua pia inaruhusika kwa sababu Malengo hua ni Kupangusia Vumbi tohara kwenye sehemu ya Wajibu ya Kiungo husika, hivyo kwa vyovyote vile itakavyowekezakana kufanikisha basi hua inaruhusika kama vile ilivyokua kwa Udhu.'**(*Al Mughni)*

Ambapo Mtu anapopiga Pigo la Kiganja chake kwenye Mchanga Tohara kwa ajili ya Tayammam basi anatakiwa apige huku akiwa amtanua vidole vyake ili vigande vumbi husika na kuna baadhi wanaweza wakajiuliza kwanini Tayammam ni Uso na mikono tu.?

Hivyo anasema Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii katika Kitabu chake cha Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii kua: **'*Allah Subhanah Wa Ta'ala* ameamrisha Kutayammam ndani ya Kitabu chake kwa kupitia katika Surat An Nisaa na Surat Al Maidah kwa kusema:**

﴿فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيداً﴾

Falam Taijiduu MaAan Fatayammamu SaAidan Tayyiban - *Na Kama Hamkupata Maji Basi Fanyeni Tayammam kwa Mchanga Uliosafi na Mzuri**(Surat An Nisaa 3:43, Surat Al Maidah 5:6)**

Hivyo kuhusiana na Fatayammamu Saaidan basi amesema kua:

﴿فَل يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَنْفِقُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا كَسَبْتُمْ وَمِمَّآ اَخْرَجْنَا لَكُمْ مِّنَ الْاَرْضِ ۖ وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيْثَ مِنْهُ تُنْفِقُوْنَ وَلَسْتُمْ بِاٰخِذِيْهِ اِلَّآ اَنْ تُغْمِضُوْا فِيْهِ ۗ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ غَنِيٌّ حَمِيْدٌ﴾

Ya ayyuhalladhîna âmanû anfiqû min thayyibâti mâ kasabtum wa mimmâ akhrajnâ lakum minal-ardh, wa lâ tayammamul-khabîtha min-hu tunfiqûna wa lastum bi'âkhidhîhi illâ an tughmidlû fîh, wa'lamû annallâha ghaniyyun ḥamîd.*(Surat Al Baqara 2:267)**

*Tafsir:****Enyi Mlioamini Toeni Kile kilichohalali na kizuri Katika Mlivyovichuma Vile tulivyokutoleeni kutoka Ardhini Na Wala Msichukue vichafu Visivyokua na Thamani Kwa Ajili ya Kuvitumia kwa Kuvitoa Ambavyo Nyinyi Hamtovipokea Isipokua Kwa Kufumba Macho Na Fahamuni kua Kwa Hakika Allah ni Tajiri Anejitosheleza na ni Mwenye Kustahiki Shukrani.***

Hivyo Maana ya Tayammam humaanisha Nia kwa ajili ya Kitu Fulani, Hivyo maana ya *FaTayammamu* basi humaanisha Tieni Nia kwa ajili ya Kitu.

Ama kuhusiana na *Saaidan* yaani Udongo au Sehemu ya juu ya Ardhi basi hua kuna maana mbili juu yake, ambapo maana ya kwanza ni kua Kila kinachoota Ardhini ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Abu Hanifa. Na maana ya pili ni Udongo, ambao ni Mtizamo wa Imam Al Shafii.

Ama kuhusiana na Tayyibati basi hua ina maana mbili ambapo ya kwanza ni Halali ambayo ni kulingana na Mtizamo wa Imam Sufyan Ath Thawry Na maana ya pili hua ni Safi ambalo ndio maana iliyokusudiwa na Aya.

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* akasema:

﴿فَٱمْسَحُواْ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِّنْهُ﴾

Famsahoo biwujoohikum wa aideekum minhu – ***Jipakeni Nyusoni Mwenu Na Mikononi Mwenu Kutokana nao.****(Surat An Nisaa 3:43, Surat Al Maidah 5:6)*

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameweka mipaka ya Kujifuta Nyuso na Mikono tu katika Tayammam, na wala hakusema Vichwa na Miguu, kwa sababu Kupangusa Vichwa kwa Vumbi hua ni Dalili ya watu walipatwa na Msiba na Vumbi hua halikosekani Miguuni Pale watu wanapokua Safarini.

Hivyo basi Kutokana na kua imeamuliwa Kua viungo vya Tayammam kua ni Uso na Mikono basi, Mtu hua anatakiwa kuanza kupangusa Uso wote kikamilifu, kwan akiwacha sehemu hata ndogo ambayo katika Kutia Udhu kwa Maji hua inatakiwa kupata Maji lakini katika Kutayamma ikawa hakuipangusa basi Tayammam yake hio hua ni Batili, na baada kukosha Uso basi ndio atakosha Mikono.

Ama kuhusiana na Mikono basi Wanazuoni aametofautiana Juu yake, kwani Imam Al Zuhri amaesema kua Unapangusa hadi Mabegani.

Ambapo mtizamo wa pili ni wa Imam Al Shafii ambae amesema katika Al Kauli ya zamani na kauli mpya kua Unapangusa kwa mikono hadi kwenye visugudi.

Na huu pia ndio Mtizamo wa Ibn Umar na Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhum* na kwa upande wa Tabiina basi ni wa Imam Said Ibn Musayyib, Said Ibn Jubayr, Al Hasan Al Basr na Muhammad Ibn Sirin. Na pia ndio Mtizamo wa Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Abu Hanifa na Wanafunzi wake wawili.

Mtizamo wa Tatu ni wa Imam Malik ambae amesema ni Wajibu kupangusa na viganja vya mikono na mikono yenyewe hadi kwenye Visugudi ambapo huu pia ndio mtizamo wa Ibn Masud na Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhum.*

Na ndio mtizamo wa Imam Ikrimah, na Imam Makhul na Imam Al Awzai, Imam Ahmad Ibn Hanbal na Is-haq Ibn Rahawayh Al Shafii.'*(Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii anaendelea kusema kua: 'I**mam Al Shafii amesema kua Tayammam hua ni Kupiga Mikono kwenye Udongo wa Ardhi yeyote iwe ni yenye Mchanga, iwe ni wenye Chumvi, Wenye Vumbi, au aina yeyote ile ya Mchanga ambao Vumbi lake litaganda Viganjani Lakini kwa Sharti la Kua Mchanga huo uwe Tohara usiokua umechanganyika na Uchafu wowote**

Hivyo Tayammam haikubaliki kwa Mchanga mwengine zaidi ya Mchanga Tohara utakaowacha Vumbi Viganjani.

Na Imam Abu Hanifa amesema kua: Tayammam hua inaruhusika kufanyika kutokana na Kitu chochote kile kitokacho Ardhini kimaumbile iwe Mchanga, Chokaa, Madini ila usiwe ni wenye kutokana na Matengenezo ya Utaalamu wa Kiibn Adam kama Unga wa Matofali,n.k

Na kwa Upande wa Imam Malik basi yeye amesema Kua Tayammam hua inaruhusika kufanyika kutokana na kitu chochote kile kitokacho Ardhi na hivyo chenye kugusana na Ardhi hata kama ikiwa kitu hicho si sehemu ya Ardhi kwa mfano Miti na Mimea inayotambaa.

Na hii ni kutokana na Uthibitisho wa Aya iliposema kua Fatayammam SaAaidan Tayyiban -Hivyo Fanyeni Tayammam kwa Kutumia Ardhi- Udongo Tohara na Safi.

Na Hivyo Udongo Hujumuisha Kinachotokana na Ardhi. **Na kwa sababu Amesema Said Ibn Musayyib kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua *amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ardhi yote imejaaliwa kwa ajili yangu kua ni sehemu ya Kusujudia na akujitoharishia.'**

Na hivyo kila kinachotokana na Ardhi hua ni sawa na Ardhi kua ni sehemu ya kusujudia basi hua kuna ulazima pia wa kinachotokana na Ardhi kua kinaweza kutumika Kujitoharishia na hivyo inaruhusika kutumia kwa kufanyia Tayammam.

Na hii ni kwa sababuaya imetumia neno Al SaAid ambalo maana yake ni Vumbi kwa Kilugha, kwani Ali Ibn Abi Talib na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhum* walipoilizwa kuhusiana na neno SaAid basi walisema kua Ni Vumbi Linalotapakaa kwenye Mikono yenu.

Ambapo kwa upande wa Imam Al Shafii yeye ametafsiri neno Al SaAaid kua ni lenye kutokana na asilo ya neno linalomaanisha Kinachotoka na kuja juu kutoka kwenye Udongo Kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'an kua:

﴿وَإِنَّا لَجَاعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيداً جُرُزاً﴾

Wa innaa la jaa'iloona maa 'alaihaa sa'eedan juruzaa - *Na kwa Hakika Tutakijaalia Kila Kilichopo Juu yake kua ni Ardhi Kame.* *(Surat Al Kahf 18:8)*

Na hivyo Kumaanisha Ardhi isiyokua na Miti wala Mimea Juu yake,hivyo hii inabatilisha hali ya kujumuisha Kila kinachotoka Juu yake.

Kisha Imam Al Mawardi anaendelea kusema kua: '**Kama ikiwa Tayammam inaruhusika kwa Kila Udongo uliokua Tohara Basi hua inaruhusika pia kwa aina tofauti za Rangi za Udongo kwani hua hakuna tofauti Udongo kua mwekundu, mweusi au mweupe n.k**

Hivyo asili ya rangi ya Udongo hua haibadilishi hukumu yake, kama ilivyokua kwa Maji yenye rangi yake ya Asili, na hivyo basi inakubalika Kutayammam hata kwa udongo Unaoliwa kama wa Khurasan na Bahri kwa sababu ni Udongo mbali ya kua Una Ladha tofauti.

Na pia inakubalika Kutayammam kwa Udongo wa Mfinyanzi kama wa Armenian, isipokua pale itakapokua Una Madini yasiyotoka ndani yake.

Na hivyo basi inakubalika pia Kutayammam kwa Udongo ambao harufu yake hubadilika baada ya Kuchanganywa na Maji na Kufinyangwa pale utakapokua Umekauka na Ukawa na Vumbi, kwani Udongo wenye Maji hua hauruhusiki Kufanyia Tayammam kwa sababu ya kua hua Hauna Vumbi. Mbali ya kua Ibn Wahb amesema kua Imam Malik ameruhusu kuutumia. *(Al Hawi Al Kabir Fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Kisha Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii anaendelea kutuambia kua: **'Kama ikiwa Mchanga umechanganyika na Manukato au Zafarani na kisha Mchanga huo ukabadilika basi hua hairuhusiki kuufanyia Tayammam.**

Lakini kama ikiwa haukubadilika basi hali ya kilochochanganishwa nacho Hua aidha ni Maji maji kama Marashi au hua ni Unga kama kama Zafarani.

Hivyo kama ikiwa ni Unyevunyevu basi hua inaruhusika kutayammam kwa sababu Umajimaji huo hua hauuzidi Mchanga na unapokauka hua umenyenyaa na mchanga, na hukmu hii hua sawia na Vitu vyenginevyo vya Maji maji, kama Siku, Maziwa n.k pale vinapochanganyika na Mchanga au Udongo Na kama ikiwa ni kilichomwagikia ni kama Unga basi kuna Mitizamo miwili juu ya kuruhusika kwake kufanya Tayammam kwenye Mchanga huo.

Na juu ya hili basi hua ni katika Kila kitu kitakachokua katika hali ya Unga unga, kama Unga, Majivu n.k ambapo kama Utakua haukuuzidi Mchanga basi Tayammam itakubalika juu yake Lakini kama ikiwa Mchanga au Udongo umezidiwa kwa wingi basi hua haikubaliki kufanya Tayammam kutokana na Mchanganyiko huo, mbali ya kua Imam Abu Is-haq Al Marwazi Al Shafii amesema kua hua inakubalika. *(Al Hawi Al Kabir Fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Ambapo kwa upande wa Imam An Nawawi basi anasema kua: **'Wanazuoni wetu wanasema bila kutofautiana kua kama ikiwa Mchanga uwe umechanganyika na uchafu kidogo au mwingi, basi hua haukubaliki kutumia kwa Tayammam. Na hii ni kwa sababu Mchanga hua ni tofauti na maji, kwani maji hua yana uwezekano wa kuondoa Najis iliyomo ndani yake.**

Hivyo As-hab wetu wametaja mfano wa Mchanga wa Makaburini na hukmu yake kua kama itakua mtu ana uhakika kua mchanga huo umefukuliwa basi mchanga huo utakua si tohara. Na kama mtu ikiwa hana uhakika kua umefukuliwa ama la basi mchanga huo utakua tohara, na hata kama ikiwa ana shaka kua umecfukuliwa basi mchanga huo bado utakua tohara kulingana na mtizamo unaokubalika zaidi.

Na kusema kwetu kua ni Tohara basi hii inamaanisha kua inauhusika kuufanyia Tayammam, kwani vyenginevyo basi itakua haufai. Lakini kama ikiwa haukufukuliwa basi hua inaruhusika hata kusali juu yake, mbai y akua kufanya hivyo hua haipendekezwi. Na hii kwa sababu ya kutokana na kua ni sehemu ya kufukiwa uchafu.'

Hata hivyo hua inaruhusika kuufanyia Tayammam kwa sababu mchangawake hua ni safi na hivyo hua nisawa na mchanga wa sehemu nyenginezo, na hii imeeleezewa wazi na Shaykh Nasir katika Al Intikhab kua ni msafi na ni mzuri.

Na Al Shafi amesema katika kitabu chake cha Al Umm kua: 'Kama ikiwa Mvua itanyesha Makaburini, basi Tayammam haitoruhusika kufanyika kwa sababu usaha wa Maiti hua umo ndani yake, na Mvua hua haiuondoa kutoka ndani yake, nah ii ndio hukmu juu ya kila kitu kitkachokua kimechanganyika na uchafu na kua kama mchanga.' *(Al Majmuu)*

Na tunaporudi kwa Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii basi tunaona kua anaendelea kutuambia katika Kitabu chake cha Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na Ulazima wa Vumbi vumbi kitakiwa kua ni lenye kuganda kwenye Viganja ili kupangusia kwenye Viungo vya Tayammam basi kuna Ulazima huo wa kua ni lenye kubakia na kiganda kwenye viganja ili kuvifanyia Tayammam viungo husika.**

Hivyo kama Mtu atapiga Mchanga na kisha ikawa hakuna vumbi vumbi lililomganda basi viganjani basi hua hairuhusiki kufanya Tayammam.

Lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi wao wanasema kua Inaruhusika kufanya Tayammam.

Hivyo kwao wao hua inaruhusika hata kama Mtu akipiyisha Mkono wake kwenye Jiwe, au Udongo Mkavu na kujipangusia hata kama Kiganja hakijakamata Vumbi lake Na hii ni Kutokana na Hadith ya Ibn Al Sammah ambae amesema kua: Nilipita mimi pembeni ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati akiwa anajisaidia Haja Ndogo, na baada ya kumaliza alijipangusia na Ukuta na akafanya Tayammam kwa ajili ya Uso na Mikono.

Ambapo Mtizamo wetu Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kutokana na Uthibitisho wa aya kua:

﴿فَٱمۡسَحُواْ بِوُجُوهِكُمۡ وَأَيۡدِيكُمۡ مِّنۡهُ﴾

famsahoo biwujoohikum wa aideekum minhu – ***Jipakeni Nyusoni Mwenu Na Mikononi Mwenu Kutokana nao.****(Surat An Nisaa 3:43, Surat Al Maidah 5:6)*

Hivyo maana iliyokua wazi hapa ni kua Inatakiwa Kujipangusa Kutokana na Vumbi lililoshikamana na Viganja, kwani kama hakuna kilichoshikamana na Viganja basi hua hakuna cha Kujipangusia kutokana nacho, na hivyo hua hairuhusiki kufanyia Tayammam.

Kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua :

جُعِلَتْ لنا الأرضُ كلُّها مَسْجِداً وجُعِلَتْ تُربَتُها لنا طَهُوراً

"Na Ardhi imejaaliwa kua ni sehemu ya Sala zetu na mchanga wake ni kwa ajili ya Toharisho letu."

Ambapo kile kisichoshikamana na kitu kinachotakiwa kutoharishwa hua hakiwezi kua kitoharisho Na kwa kua Hitajio ni kujitoharisha kutokana na Uchafu wa Kimwili basi hua kuna ulazima wa kupatikana njia ya Kujitoharisha kama Udhu. Na kwa kua Kitoharisho kinapangusiwa kwenye sehemu inayotakiwa kutoharishwa basi hua kuna ulazima wa kinachotoharisha kushikana na sehemu inayotoharishwa.

Na kuhusiana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kujipangusia Ukuta basi Ukuta kwa kawaida hua una Vumbi, na atakaejifutia nao hua hakosi vumbi. Kama tulivyoona katika Hadith ya Ammar ambae alisema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baada ya kupiga mikono alipuliza Viganja vyake na hii ni kwa sababu kupuliza hua kunaondoa Vumbi lakini hakuondoi vumbi lote.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipuliza Viganja kisha akajipangusia Uso kwa sababu nia yake ni kumfundisha Ammar kufanya Tayammam, na kufanya Tayammam kwa ajili yake binafsi na hivyo wingi wa Vumbi lililobakia katika Viganja vyake baada ya Kupulizia lilitosheleza Kufundisha kufanya Tayammam.'*(Al Hawi Al Kabir Fi Fkqh Madhhab Al Shafii)*

Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii anaendelea kutufahamaisha zaidi namna ya kufanya Tayammam kwa kusema kua: **'Imam Al Shafii amesema kua: 'Mtu anatakiwa kupiga mkono wake kwenye mchanga huku akiwa ametawanya vidole vyake, hadi ahakikishe kua vimejaa vumbi. Na akisha anajipangusia Usoni na mikono yae hio, na kisha anapiga tena pigo jengine katika njia hio hio na kisha anaipangusa sehemu ya nyuma ya mkono wake wa kulia Pamoja na vidole vyake kuelekea kwenye kisugudi cha mkono huo kwa kutumia kiganja chake cha mkono wa kushoto na kisha anaugeuzia upande wa ndani wa mkono huo wa kulia na kuupangusa kuanzia kisugudini hadi kwenye vidole vyake vya mkono huo hadi kwenye ddole gumba huku akiwa hakuacha sehemu yeyote ya mkono huo katika kuupangusa kwake. Na kisha anafanya hivyo hivyo kwa mkono wake wa kushoto kwa kutumia kiganja chake cha mkono wake wa kulia''**

Na watu wametofautiana kuhusiana na idadi ya mapigo ya kupangusa uso na mikono, kwani amesema Imam Ibn Sirin kua mapigo yasiyopungua matatu hua hayatoshelezi. Yaani pigo moja ni kwa ajili ya uso, la pili kwa ajili ya vinganja na la tatu kwa ajili ya mikono. Ambapo kwa upande wa Is-haq Ibn Rahawayh basi yeye amesema kua Pigo moja tu linatosheleza ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi chini ya mapigo mawili hua haitoshelezi kufanya Tayammam, yaani moja kwa ajili ya uso na la pili kwa ajili ya mikono.

Na hii ni kulingana na hadithi ya Salim ambae amesema kua amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:'' Katika Tayammam basi yanahitajika mapigo mawili, ambapo Moja ni kwa ajili ya Uso na jengine ni kwa ajili ya Mikono hadi kwenye visugudi'

Na Urwa Ibn Thabit amesema kua amesema Abu Zubayr kua amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allah Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Tayammam hua ni Pigo Moja la Uso na pigo moja kwa ajili ya Mikono hadi kwenye visugudi'

Na kama ikiwa imethibitishwa kua mapigo mawili yanatosheleza na chini ya hapo kiidadi hua hayatoshelezi basi Al Shafii amesema kua: 'Mtu anatakiwa kupiga mikono kwenye Vumbi kwa mikono yake na kutawanya vidole vyake hadi vumbi litawanyike na kujaa kwenye vidole lake, lakini hata hivyo kupiga mikono kwenye vumbi hua si sharti bali kinachotakiwa ni kua Vumbi lishikamane na Kiganja, hivyo kama akiweka kiganja chake na kutawanya vidole vyake na vumbi likashikamana navyo basi hua inaruhusika kufanya hivyo, na kama ikiwa halishikamani na basi hapo ndio itambidi kupiga hadi pale litakaposhikamana na viganja vyake.'

'Ama kuhusiana na kutanua vidole basi vumbi hilo linatakiwa liingie hadi kwenye baina ya vidole vyake na hivyo hua ni wajibu, hivyo kama akipiga mchanga na kisha Vumbi likamganda basi Al Zafarani basi amemnukuu Imam Al Shafii katika Al Qawl Al Qadim ikisema kua: 'Inapendekezwa kupulizia Viganja baada ya kupiga kwenye mchanga, lakini katika Al Qawl Al Jadid basi imesemwa kua haipendekezwi, hivyo baadhi ya As-hab wetu wametafsiri mitizamo miwili hii kutokana na utofauti wake katika sehemu mbili hizo.'

Imam Al Shafii amesema kua: 'Mtu hua anatakiwa kupangusa viganja vyake viwili na kuvishikamanisha vidole vyake.'

Ama kuhusiana na kupangusia kiganja kimoja kwenye kiganja chengine basi kuna mitizamo miwili juu yake. Ambapo Mtizamo wa kwanza ni kua hua inapendekezwa na hii ni kwa sababu Vumbi hua limegusa sehemu zote hivyo haina haja ya kupangusa kama Maji.

Mtizamo wa pili ni kua hua ni Wajibu kupangusia kwa sababu Vumbi hua ni tofauti na maji ambayo hua yanamiminika kimaumbule na kufikia kila sehemu ya kiungo husika, ambapo hali hii hua haipatikani katika mchanga, ambao una maumbile ya ugumu na hivyo hua haufikii kwenye vifundo isipokua kwa kupangusia kwenye kiungo husika.

Ama kuhusiana na kushikamanisha Vidole basi kama ikiwa Vumbi halikufikia baina ya Vidole viwili, basi kuvishikamanisha hua ni wajibu lakini kama ikiwa limefikia shemu hizo basi hua kuna mitizamo miwli juu yake kama tulivyosema.

Na kama ikiwa watu watahoji kwanini Al Shafii akasimamia kwenye kuielezea Tayammam kua ni mapigo mawili kama alivyosema, basi kuna mitizamo miwili juu yake, ambapo kwanza ni kua katika hili basi Al Shafii amefuata Mtizamo wa Hadith ya *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam.*

Na pili ni kwa sababu y akua ni mwenye kujibu suli la wale ambao watasema kua pigo moja hua halitoshelezi. Hivyo Al Shafii akaelezea kukubalika kwake na kuelezea juu ya kutowezekana kwake, hivyo kama mapigo mawili hayajatosha basi itambidi mtu apige pigo la tatu na la nne hadi ahakikishe kua Uso wote na mikono yote umeguswa na vumbi. Ambapo katika Mtizamo wake wa zamani Imam Al Shafi amesema kua: 'Kupulizia Mikono hua ni Sunnah, na hii ni kwa sababu Ammar Ibn Yasir amenukuu kutoka kwa *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam.'*

Na mtizamo wa pili ni kua amesema katika Mtizamo wa Al Qawl Al Jadid kua si Sunnah na Jabir amenukuu hadithi hio. Na wengine miongoni mwa As-hab wetu wamesema kua hili halitegemeani kulingana na mitizamo miwili bali hua linategemeana kulingana na hali mbili tofauti za kimazingira hivyo katika Al Qawl al Qadim Imam Al Shafii amesema kua inapendekezwa kupuliza kutokana na kua kama vumbi lililoshikamana na Viganja ni jingi sana. Hivyo Sunna hua nikulipuliza ili lile atakalo jipangusia katika kutayammam liwe kidogo, ambapo mtizamo huu hua si sahih.

Na katika Al Qawl Al Jadid amesema kua: 'Inapendekezwa kutopulizia kutokana na ukweli wa kua kama ikiwa vumbi lililoshikamana na viganja ni kidogo hivyo kama mtu akipulizia viganja baada ya kuvipiga mchangani basi atakue hakubakisha Vumbi kwenye viganja kwa ajili ya Tayammam yake hio.'

Kisha Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii anaendelea kutuambia katika Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii kua: '**Amesema Imam Al Shafii kua Anaetaka Kusali na akakosa Maji ya Udhu na Kutayammam basi hua ni mwenye Wajibu wa Kunuia Kusali kwa Kutayammam, na huu ndio Mtizamo Sahih.'**

Hivyo Nia katika Kufanya Tayammam hua ni Wajibu, na juu ya hili la kua ni Wajibu basi wanakubaliana Imam Abu Hanifa na Imam Malik. Hivyo basi kukubaliana kwako hakumpelekei Mtu Husika kua Tohara kutokana na Najis aliyokua nayo, bali hua kunampelekea Mtu husika kua ni mwenye Kuruhusika kufanya Ibada ya Sala.

Na Mbali ya kua kukubaliana kwao kua Tayammam inamruhusu Mtu kufanya Ibada, lakini hapo hapo wametofautiana kuhusiana na Utohara wa Mhusika. Kwani Imam Abu Hanifa anasema kua Tayammam inaondoa Uchafu wa Najis kama vile unavyoondoa Udhu kwa kutumia Maji na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kutoka kwa Ayun, kutoka kwa Abu Qilabah kutoka kwa Mtu wa Banu Amr kutoka kwa Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*: 'Ardhi Safi ni Tohara na aimejaaliwa kua Kitoharisho.''

Hivyo Abu Hanifa anasema kua kutokana na kua Ardhi ni Kitoharisho cha Uchafu na ni Wajibu kutokana na kua inaruhusu utekelezwaji wa Ibada ya Sala, na hivyo Tayammam hunufaisha kwa kuondoa uchafu kama ufanyavyo Udhu.

Kwani Tayammam ni Moja kati ya Njia mbili za Kujitoharisha, na hivyo inawajibu wa kutoharisha kama yalivyo Maji, hivyo basi kama ingekua Tayammam haitoharishi basi isingekua na uwezo wa kubatilika, ambapo hubatilika kutokana na kuwepo kwa Uchafu baada ya kufanywa kwake.

Imam Al Mawardi Al Shafii anaendelea kusema kua: **'Lakini Uthibitisho wetu sisi wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, ni kua Tayammam hufanywa kutokana na Dharurah ya kutakiwa**

kupatikana Utohara, mbali ya kua Uchafu haujaondoka, yaani hii inakua kama hali ya Mwanamke mwenye Istihadhah.

Na ndio maana Mtu atakaetayammam basi akipata Maji atatakiwa Kujitohariaha Upya,na hii ni kutokana na kua ni bado mwenye kua na Uchafu Kama vile yule anaeruhusika Kusali bila ya Kua na Maji au Mchanga, na hivyo hua ni mwenye kua na Wajibu wa Kujitoharisha pale atakapopata Maji, na hivyo Utohara wake Mtu huyu hua hauko sawa na wa Mtu mwenye Kutia Udhu kwa Maji.

Na kwa kama ikiwa Mtu husika hua anakua tohara kutokana na Tayammam sawia na Mtu alietia Udhu basi asingetakiwa Kutia Udhu pale atakapopata Maji katika Sala za vipindi vitakavyofuatia, kama vile amavyoruhusika mwenye kua na Udhu Utokanao na Maji.

Ama kuhusiana na makisio ya kua ni sawa na Udhu basi maana yake ni kua Udhu hua unahitajika kutumika kwa maji yatakapopatikana na hivyo hii hua inamaanisha kua Uchafu husika hua unaondoka kutokana na Maji.

Hivyo kutokana na kua Mtu atatakiwa Kujitohariasha upya akipata Maji basi hii inamaanisha kua Uchafu ulikua bado upo. Hivyo Maji hua yanatumika kutokana na kutokuwepo kwa Dharurah ya kukosekana kwa Maji Hivyo kama ikiwa Mtu ana Janaba kisha akafanya Tayammam kwa Nia ya Janaba,na kisha Utohara wake ukabatilika kutokana na Najis ndogo na kisha akaona Maji, basi Mtu huyo huwajibika Kukoga Janaba kwanza.

Kwani kama ingekua Tayammam imemtoharisha na Janaba basi asingekua na Wajibu wa Kukoga Janaba baada ya kupatwa na Najis Ndogo, na hivyo angetakiwa ajitoharishe kwa ajili ya Najis ndogo tu. Ambapo huu ndio uthibitisho wenye Nguvu wenye kuonesha kuendelea kuwepo kwa Uchafu wa Awali baada ya Tayammam.

Kwani Tayammam ya mtu hua inabatilika kutokana na Najis inayofuatia baada ya kutayammam kwakwe kwa sababu Tayammam hua Inamruhusu Mtu kusali kutokana na Najis ya Awali hapo kabla na wala si kutokana na Najis itakayofuata.' *(Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Hapa tunaona kua Mfano alioutoa Imam Al Mawardi hapa ni kua kwa Mfano Mtu ulikua na Janaba na ukakosa Maji basi Utatia nia ya kujitojarisha Janaba, na kisha Uweza kusali pia.

Lakini kama Udhu ukikutoka kwa kujisaidia,Kugusana na Wanawake n.k na kisha Ukakuta Maji basi hutoruhusika Kusali kwa kutia Udhu peke yake tu bali itakubidi ujitoharishe upya kwa kukoga Janaba kwanza kabla ya kuendelea na Udhu wa Ibada ya Sala inayofuatia.

Hivyo Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii anaendelea kutuambia katika Kitabu chake cha Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii kua: **'Amesema Mmoja kati ya Watu wa Banu Amir aitwae Amr Ibn Budjan kua:**

دخلتُ في الإسلامِ فأهَمَّني ديني فأتيتُ أبا ذرٍّ فقالَ أبو ذرٍّ إنِّي اجتويتُ المدينةَ فأمرَ لي رسولُ اللَّهِ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ بذَودٍ وبغنَمٍ فقالَ لي اشرب من ألبانِها – قالَ حمَّادٌ وأشُكُّ في أبوالِها هذا قولُ حمَّادٍ – فقالَ أبو ذرٍّ فَكُنتُ أعزُبُ عنِ الماءِ ومعي أهْلي فتصيبُني الجَنابةُ فأصلِّي بغيرِ طَهورٍ فأتيتُ

رسولَ اللَّهِ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ بنصفِ النَّهارِ وَهوَ في رَهْطٍ من أصحابِهِ وَهوَ في ظلِّ المسجِدِ فقالَ أبو ذرٍّ فقلتُ نعَم. هلَكْتُ يا رسولَ اللَّهِ قالَ وما أهْلَكَكَ قلتُ إنِّي كنتُ أعزُبُ عنِ الماءِ ومعي أهْلي فتصيبُني الجَنابةُ فأصلِّي بغيرِ طُهورٍ فأمرَ لي رسولُ اللَّهِ صلّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ بماءٍ فجاءت بهِ جاريةٌ سوداءُ بعُسٍّ يتخَضخَضُ ما هوَ بملآنَ فتستَّرتُ إلى بعيري فاغتسلتُ ثمَّ جئتُ فقالَ رسولُ اللَّهِ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ يا أبا ذرٍّ إنَّ الصَّعيدَ الطَّيِّبَ طَهورٌ وإن لم تجدِ الماءَ إلى عشرِ سِنينَ فإذا وجدتَ الماءَ فأمسَّهُ جِلدَكَ

Niliingia Katika Dini ya Uislam hivyo nikaenda kwa Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu* na Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu* akasema kua : 'Nilikuja Mimi katika Mji wa Madina na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaagizia Ngamia na Kondoo kwa ajili yang una kuniambia: 'Kunywa Maziwa yake' Hammad akasema: 'Ama Mimi nashukia Mkojo wake' na hivi ndivyo alivyosema Hammad'

Akasema Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu* kua: Mimi nilikua ni Mtu ambae niko mbali na sehemu yenye Maji, na Familia yangu ilikua pamoja nami. Na ilikua kuna wakati ambao nnakua sina Tohara, na hivyo nikawa nnasali bila ya kujitoharisha.

Hivyo nikaja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumlalamikia kwa kumwambia: 'Ya Rasul Allah hakika mimi Nimeshaangamia!'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akauliza : 'Jee ni Kitu gani kilichotokea na kukupelekea kuangamia?'**

Nami nikamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Mimi pamoja na familia yangu nilikua katika sehemu ambayo haina Maji, na kuna wakati ikawa sina Tohara, hivyo imenibidi niwe nasali bila ya Kujitoharisha.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaniamrisha nichukue Maji kisha Nikoge, na hivyo nikajitoharisha, na kuenda kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae akaniambia kua: 'Ewe Abu Dhar! Kwa Hakika Ardhi Ni Tohara hata kama ikiwa hukupata Maji kwa mda wa Miaka 10, Ila Ukipata Maji basi wacha Ngozi yako Iyaguse Maji hayo.'

Ambapo Hadith hii na nyenginezo zinadhihirisha kua inaruhusika Kufanya Tayammam hata kwa Mtu mwenye Janaba.'

Ambapo kabla ya kuandelea basi tunakumbushana kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Wanasema kua Tayammam Haiondoi Uchafu wa Mwili, kama yafanyavyo Maji, hivyo Tayammam hua kwa ni Dharurah tu inayokupelekea Kuruhusika Kusali Na ndio Maana hua inatakiwa Kama Mtu umefanya Tayammam kwa kukosa Maji, na kisha Ukaona Maji basi Tayammam yako hua Inabatilika na hivyo itakubidi Ujitoharishe kwa Maji hayo uliyoyaona.

TAYAMMAM NA HUKMU ZAKE

❖❖❖❖

Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii ambae alizaliwa Mwaka 972 C.E na kufariki Mwaka 1058 C.E aliozaliwa Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii Al Tusi. Na mbali ya Kua ameishi Miaka 1000 iliyopita lakini Alhamd lillah anatunufaisha juu ya Hukmu za Tayammam kama alivyoelezea katika Kitabu chake cha Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii kwa kusema kua: **'Kama Ikiwa kuna uthibitisho kua Tayammam haiondoi Uchafu, na Kua Nia ya Tayammam ni Wajibu basi juu ya hili kuna hali zifuatazo Katika Nia:**

'Kwanza - Mtu kama Mtu atanuia katika Tayammam Yake kua Anajitoharisha kwa ajili ya Kuondoa Uchafu wa Mwili, basi Tayammam yake Itakua Batili.

Na hii ni kwa sababu Tayammam haitoharishi, na hivyo kutokana na uhalisia huu basi Nia ya Mtu itakua inapingana na Hukmu ya Tayammam ma hivyo Tayammam hio hua ni Batili. Mbali ya kua baadhi ya Wenzetu wanasema kua Tayammam yake inakua Sahih kwa sababu maana ya Nia ya kuondoa Uchafu hua ni kuifanya Sala iruhusike, na Tayammam huifanya Sala iruhusike Hata Kama Uchafu haunaondoka.

Pili - Kama Mtu atanuia katika Tayammam yake kua ni Kuifanya Sala iruhusike, basi Tayammam yake itakua Sahih lakini si kwa Sala za Faradhi.

Na hii ni kwa sababu Tayammam huzifanya Sala za Sunna kuruhusika bila kuziainisha katika Kunuia kwake, lakini kwa upande wa Sala za Faradhi basi hua hairuhusiki hadi Izianishe katika Nia ya Tayammam.

Na pia haitoruhusika kufanya Tawwaf kwa Mtu husika alietia nia ya Tayammam ya Kuruhusika Kusali, kwa sababu Tawwaf hua si Sala, na kutokana na kua hakuijumuisha Tawaf katika Nia yake ya Tayammam ya kuomba Kuruhusika Kusali.

Hivyo Suali linakuja Jee itaruhusika kwa Mtu huyu kusali Rakaa mbili za Tawwaf kwa Nia hio?

Na Jibu la Suali hili lina mitizamo miwili tofauti, ambapo kwanza inabidi kujua Jee Rakaa hizo za Tawwaf ni Fardhi au ni Sunna?

Ambapo kama ikiwa ni za Fardhi basi hua hairuhusiki Kuzisali, lakini kama ikiwa ni Sunnah basi itaruhusika, na itaruhusika pia kubeba Msahafu na kusoma Qur'an, kwani hivi hua ni Tofauti na Tawwaf ambayo hua ni vitendo vya Kiibada.

Tatu- Kama Ikiwa Mtu atanuia Kutayammam kwa ajili ya Sala ya Sunnah, basi ataruhusika Kusali ndani yake Tayammam hio Rakaa atakazo za Sunnah, lakini Kamwe hatoruhusika Kusali Sala ya Fardhi.

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Hanifa basi yeye amesema kua: Inaruhusika kwa Mtu atakaenuia Tayammam ya Sala za Sunnah kusali Sala za Fardhi pia, na hii ni kwa sababu Tohara ya Sala ya Sunnah inaruhusu pia kusalia Sala ya Fardhi kama ulivyo Udhu, kwani kila Sala inayokubalika ya Mtu alietia Udhu hua ni yenye kukubalika pia kwa alietayammam.

Ambapo Uthibitisho wetu sisi Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni kua Haikubaliki kwa sababu Mtu husika amefanya Tayammam bila ya Kutia Nia ya kua ni Kuomba Kuruhusika Kusali Sala ya Fardhi,hivyo haikubaliki kusali Sala Ya Fardhi kwa kutokana nayo, ambapo hii hua ni sawa na Kufanya Tayammam bila kunuia*' (Al Hawi Al Kabir fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Imam Al Mawardi anaendelea kutuambia kua: '**Hivyo haikubaliki Kutayammam bila kunuia Ibada ya Fardhi hivyo hua hairuhusiki kutekeleza Ibada ya Fardhi kutokana nayo Tayammam hio, kwani hua ni sawa na Mtu alietayammam bila Kutia Nia.**

Kisha Imam Al Mawardi anaingia kwenye ufafanuzi wa Hoja kwa kutumia Ilm Al Mantiq kwa kutuambia kua: Ambapo inasemwa kua Hoja juu ya Jambo hili hua zinasimamia katika Kanuni Mbili:

Kanuni ya kwanza ni kua Tayammam haiondoi Najis, na juu ya hilo basi tayari tumeshalizungumzia, Hivyo kama haiondoi Najis basi Nia hua ni kutokana na kuomba Ruhusa inayotakiwa kutokana nayo na hivyo Nia hio hua ni Nia yenye Umaalum wa Kitendo cha Ibada husika. Na kama ikiwa kuna umuhimu wa Kuainisha Nia ya Kuruhusika kwa Ibada husika basi hua haikubaliki.

Hua na Uzito sawia na hivyo hakuna yenye Uzito mwepesi zaidi Kihukumu baina yao, na Ibada ya Fardhi hua haiwi na wepesi Kihukumu zaid ya Ibada ya Sunnah. Ama kuhusiana na makisio yake hali hii na Udhu basi ni kua Udhu hua ni Utoharishaji usiokua wa Dharurah, hivyo Udhu kihukumu hua una Uzito katika utekelezaji Ibada ya Sala ya Fardhi kulingana na Tayammam ya Ibadah ya Sunnah.

Lakini kwa upande wa Tayammam basi hua ni Utoharishaji wa Dharurah na hua na Uwepesi Kihukumu kwa utekelezaji Sala ya Faradhi kulingana na Tayammam ya ya Sunnah. Ambapo kama tukilinganisha hii na Sala ya Sunnah basi sisi hatuzuii Mtu kusali Sala ya Fardhi kwa Tayammam pale itakapokua Mtu amenuia ndani yake Sala hio ya Fardhi, ila tunasema kua inatakiwa iwe ni yenye Kunuiwa Ipasavyo kihukumu.

Kwa maana hio basi Sala ya Sunnah ni Nyepesi Kimasharti na hivyo inaruhusika kusaliwa kwa Tayammam ambayo haikunuiliwa ndani yake, Na Sala ya Fardhi ni nzito kimasharti kiasi ya kua hua haikubaliki kusaliwa kwa Tayammam ambayo haikunuiliwa nia yake ndani yake kwa Ajili yake.

Hali ya Nne ni kua Kama Mtu atanuia Kutayammam kwa ajili ya Sala ya Faradhi basi Tayammam hio itamtosheleza kwa Sala ya Fardhi husika na kwa Sala za Sunnah zake ndani ya wakati huo.'*(Al Hawi Al Kabir Fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Na anasema pia Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Nia ya Kutayammam hua ni Wajibu katika Skuli ya Madhhab yetu ya Al Shafii na juu ya hili halina kupingana juu yake, na hali iko hivyo hivyo pia kwa upande wa Udhu na upande wa Kogo la Janaba.**

Na Mtizamo wa Wanazuoni na Vithibitsho vyao juu ya hili na matawi yake basi tayari Vimeshazungumziwa katika Mada ya Nia ya Udhu.

Ama kuhusiana na Ufafanuzi wa Nia ya Tayammam basi ni kua: Kwa hakika kama ikiwa mtu amenuia kuifanya Sala iruhusike juu yake, basi Tayammam yake itakua ni Sahih bila ya kuwepo

kutokukubaliana juu ya hili, na hii ni kwa sababu ya kua Mtu Husika hua ametia Nia kulingana na Inavyotakiwa.

Lakini kama ikiwa atakua ametia ni ya Kujitoharisha, basi hapa hua ni kulingana na Jawabu la suali la kua Jee Tayammam Inamtoharisha Mtu ama la.

Na juu ya Suali hili basi kuna Majibu Mawili, ambapo kwanza ni kulingana na Mtizamo uliokua Sahih Kabisa ambao ni kua Tayammam haimtoharishi Mtu, na huu ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni.

Na Mtizamo wa pili ambao ni Mtizamo wa Imam Abu Abbas Ibn Surayj ambae amesema kua: 'Tayammam Humtoharisha Mtu kwa ajili ya Sala moja Tu.'

Na Uthibitiaho wa Madhhab yetu ni kulingana na Hadith ya Imran Ibn Husayn *Radhi Allahu Anhu*, ambae alikua na Janaba na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuamrisha kua Akoge Janaba atakapopata Maji.

Na pia kutokana na Hadith ya Abu Dhar ambae aliambiwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Mchanga Msafi ndio Udhu wa Muislam, hivyo akipata Maji basi na wacha Maji hayo yaiguse Ngozi yake. Na Hadith ya Amr Ibn Al As *Radhi Allahu Anhu* ambae aliambiwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Umewasalisha wenzako wakati Ukiwa na Janaba.

Ambapo Hadith zote hizi zinaonesha kua Tayammam haiondoi hali ya Janaba, kwa sababu kama ingekua Inaondoa basi isingehitajika Kukoga Janaba kwa Maji. Ambapo Imam Al Haramayn amesema kua: Hadith aliuoizungumzia Ibn Surayj ni dhaifu na ni yenye kubeba kasoro kwa sababu uondoaji wa Janaba hua ni kwa Mwili mzima, na wala hauwi kwa ajili ya sehemu tu ya mwili.

Hivyo kama tukichukua Mtizamo wa Ibn Surayj kua Mtu atanuia Kuondoa Janaba Tu, basi Tayammam yake itakua Sahih.

Lakini kama tukichukua Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hapa itakua kuna hali mbili, ambapo hali ya Mtizamo wa pili ndio sahih zaidi ambao ni wa kua Tayammam hio hua si Sahih, na huu ndio Mtizamo wa Madhhab kulingana na Makubaliano ya Qadhi Abu Tayyib na Wanazuoni wetu.

Na kuna Mtizamo wa pili kuhusiana na Kama Tayammam inamtoharisha Mtu ama la, ambao ni ule Mtizamo usemao kua Tayamamm inamtoharisha Mtu.

Ambapo huu ni Mtizamo wa Ibn Khairan, na ni Mtizamo wa kustaajabisha na dhaifu kabisa, kwa sababu kama ikiwa Mtu ana Janaba na kisha akafanya Tayammam kwa nia ya Kujitoharisha Janaba, kisha akanuia Kujitoharisha na Najis ndogo kama vile anavyonuia anaejitoharisha mtu na Najis ndogo, basi kama itakua amenuia Kujitoharisha kutokana na Janaba basi Tayammam hio hua ni Batili kama vile ambavyo alivyonuia kujitoharisha kwa Najis ndogo.

Na juu ya hili imeamuliwa na Al Qadhi Abu Tayyib, Imam Ibn Al Sabagh, Imam Al Ruwayni na Shaykh Nasir, w Allahu Aalam.'

Hivyo Tayammam haitoharishi kulingana na Mtizamo wetu Wengi miongoni mwa Wanazuoni. **Na kulingana na Mtizamo wa Daud, Al Kharki Al Hanafi na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi ni kua Tayammam hua inatoharisha.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Hivyo Tayammam hua ni batili pale inapofanywa bila ya Nia, na juu ya hili kuna Makubaliano ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Malik, Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal, na ndio pia Mtizamo wa Ibn Hazm, na Maimamu wa Tabiina na pia. Kuna Makubaliano ya Wanazuoni Juu ya Jambo hili kama livyothibitishwa na Imam Abu Bakr Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii, Imam Ibn Hazim, Imam Ibn Abd Al Barr, Imam Ibn Rushd, Imam Al Qarafi na Imam Ash Shanqiti.

Ambapo tunapozungumzia kuhusiana na Niyyah ya Tayammam basi tunaona kua ni kama alivyoelezea Imam Al Mawardi Al Shafii katika Mifano na Ufafanuzi wa hali tofauti, ila kwa kukumbushana kuhusiana na Nia basi ni Kua Nia juu ya Kila Kitu hua ni Kuanzia Moyoni mwa mtu juu ya Amali au Ibada husika.

Na Wanazuoni wanasema kua Nia ya Moyoni hua inatosheleza ila hua ni vizuri zaid pia Kutamka kwa Ulimi Kama ni sehemu ya kujikumbusha ndani ya Nafsi yako kwa kusema kwa sauti ya kujisiki wewe mwenyewe kua Umeingia ndani ya Amali kufanya husika au Ibada husika. Na Nia ya Tayammam ya Ibada ya Sala hua si Kujitoharisha bali hua ni Kuomba Kuruhusika Kuingia Ndani ya Ibada ya Sala husika kwa mfano kwa kusema: **'Nanuia Kufanya Tayammam kwa ajili ya Kuruhusika Kusali Salat Al Fajr, au Dhuhr n.k.'**

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kua Kama Utasali Al mbili za Fardhi katika wakati mmoja basi itakubidi uzisali kwa kufanya Tayammam tofauti mbili yaani kwa kila Sala na Tayammam yake.

Ama kwa upande mwengine basi anasema Imam Al Buhuti Al Hanbali kua: **Hua ni Lazima Kuainisha Nia ya Tayammam juu ya kitu unachokifanyia Tayammam, kwa mfano Sala, Tawwaf, Kusoma Qur'an, Tohara ya Janaba, Tohara ya Najis Ndogo ndogo, n.k**

Na hii ni kwa sababu Tayammam haiondoi Najis husika bali hua ni yenye kuifanya Ibada ya Sala kua Ni yenye kuruhusika, hivyo hakuna njia nyengine ya kuipa nguvu Tayammam kutokana na Udhaifu wake.

Ambapo njia ya Kuainisha Tayammam kwa ibada husika hua ni kusema kwa mfano Ni Kutayammam kwa Ajili ya Kuruhusika Kusali Sala ya Adh Dhuhr, au kutokana na Janaba, au kutokana na Najis ndogo, au pia kunuia kwa ajili ya Janaba na Najis ndogo, au kwa ajili ya yote yaani kwa Janaba, kwa Najis Ndogo na kwa Kruhusika Kusali pia, hivyo Janaba hua inakubalika kwa Vyote pia kwa pamoja kutokana na Ujumla wa Jumuisho lake, ila nia yake akiainisha jambo moja tu basi Tayammam hio haitofaa kwa jambo jengine isipokua kwa hilo tu aliloliainisha.

Na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambayo amesema kua: Kwa Kila Mtu atalipwa kutokana na alichokinuia. **Hivyo Kama Mtu akinuia kwa ajili ya Janaba tu, basi haiwezekani kua asali kwa Tayammam hio mwa sababu hakuinilia kwa ajili ya Tayammam yake hio**. **Na akinuia kwa ajili ya Kusoma Qur'an Mskitini basi ataruhusika lakini hatoruhusika Kusali kutokana na Tayammam hio n.k.**'*(Kashhaf Al Qina)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Kharashi Al Maliki basi yeye amesema kua: '**Mtu afanyae Tayammam ni lazima awe na nia ya Kuifanya Ibada ya Sala iruhusike kwake au kama ikiwa ana**

Najis ndogo basi Nia kwa ajili ya Naji ndogo au Janaba kwa ajili ya Janaba, kua na nia ni lazima.'*(Mukhstar Al Khalili)*

Naam anasema Imam Al Shurunbulali Al Hanafi kua: **'Ni lazima kwa mtu mwenye kufanya Tayammam kutia Nia ya Kuifanya Sala yake kua ni yenye kuruhusika, iwe ni kutokana na kua na Janaba au kua na Najis ndogo. Na Nia hua inaanza kutiwa pale Mtu anapopiga Mikono yake kwenye Mchanga'***(Maraqi Al Falah)*

Ambapo anasema Imam Ibn Hazim Al Andalus katika kitabu chake cha Al Muhallah kua: '**Mtu anaefanya Tayammam anaweza Kusali Sala anazozitaka za Fardhi pale itakapokua Tayammam yake haijabatilika kwa Janaba, Najis ndogo au Kupata Maji**. **Ambapo kwa Mtu Mgonjwa basi Tayammam yake hua haibatiliki isipokua kwa kile inachobatilisha Udhu**. **Ambapo huu ndio Mtizamo wa Imam Abu Hanifa, Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Al Layth Ibn Saad na Daud.**

Na pia amesema Hammad Ibn Salamah kua amesema Yunus Ibn Ubayd kua amesema Al Hasan kua: Mtu anaweza Kusali Sala zote kwa Tayammam moja kama ilivyokua kwa mwenye Udhu pale itakapokua haijabatilika Tayammam yake hio. Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Imam Al Zuhri, na Imam Qatadah, Imam Said Ibn Musayyib na Yazid Ibn Harun.

Na amesema Muhammad Ibn Ali, na Imam Malik Ibn Anas kua: Sala Mbili za fardhi hua haziwezekani Kusaliwa kwa Tayammam moja. Kwani Mtu anatakiwa Asali Sala tofauti za Fardhi kwa Tayammam tofauti, ila Itakubalika kama Atasali Sala ya Fardhi na kisha Sala ya Sunnah kwa Tayammam hio hio moja.

Na Al Shafii amesema kua: Hua kuna ulazima kwa Mwenye Kufanya Tayammam kua afanye Tayammam kaa Kila Sala ya Fardhi, ila anaweza pia Kusali Sala ya Sunnah kabla ya Sala hio ya Fardhi na hata Baada ya Sala ya Fardhi husika. Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Sharik, Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Ash Shaabi, Imam Rabiah, Imam Qatadah Ibn Diyama Al Sadusi na Imam Yahya Ibn Said Al Ansari. Na pia ndio Mtizamo wa Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Ahmaf Ibn Hanbal na Imam Is-haq Ibn Rahawayn.

Ambapo kwa Imam Abu Thawr Al Shafii basi amesema kua: Mtu atakaefanya Tayammam hua na Wajibu wa Kufanya Tayammam kwa kila Sala ya Fardhi atakayoisali isipokua anaweza Kusali Zala za Kadhaa zote kwa Tayammam hio hio Moja.'*(Al Muhallah)*

Na amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua**: 'Wengi Miongoni mwa Wanazuoni wetu wa Madhhab ya Al Shafii wamesema kua: Ni Wajibu kuchanganya Sala Sala kwa wale Watakaofanya Tayammam na Hakuna Tatizo baina ya Mda utakaokuwepo kutayammam tena baina Kuchanganya Sala ya kwanza na ya Pili.'** *(Al Majmuu Sharh Muhadhdhab)*

Na akasema Imam Abd Rahman Ibn Muhammad Awadh Al Jazari katika Fiqh Al Madhahib Al Arbaa kua: '**Katika Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua kuhusiana na Kuchanganya Sala kwa Mtu mwenye Dharurah ya kuchanganya Sala Mbili kwa pamoja bila ya kua na Tofauti kubwa ya wakati baina ya Sala mbili husika, na bila kusali Sala za Sunnah baina yake.**

Hua inakubalika Kuzitofautisha kwa Kuadhini na kukimu Sala baina yake na Kutia Udhu, basi kwa Mtu mwenye Tayammam hua anaruhusika kuchanganya Salat Al Dhuhr na Salat Al Asr kwa kutayammam baina ya Sala mbili hizo kwa sababu hua hairuhusiki kuchanganya Sala mbili kwa Tayammam moja.'*(Fiqh Aala Madhahib Al Arbaa)*

Na kuna hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ فُضَيْلٍ، عَنْ أَبِي مَالِكٍ الأَشْجَعِيِّ، عَنْ رِبْعِيٍّ، حُذَيْفَةَ، عَنْ حُذَيْفَةَ فُضِّلْنَا عَلَى النَّاسِ بِثَلاَثٍ جُعِلَتْ صُفُوفُنَا كَصُفُوفِ قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم الْمَلاَئِكَةِ وَجُعِلَتْ لَنَا الأَرْضُ كُلُّهَا مَسْجِدًا وَجُعِلَتْ تُرْبَتُهَا لَنَا طَهُورًا إِذَا لَمْ نَجِدِ الْمَاءَ " وَذَكَرَ خَصْلَةً أُخْرَى

Amesema Abu Bakr Ibn Abi Shaybah kua amesema Muhamamd Ibn Fudhayli kua amesema Abu Maliki Al AshjaAi kua amesema Al Rabii kua amesema Hudhayfah *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Hakika Sisi Tumefadhiliwa kwa kupendelewa Mambo matatu:

1-Safu zetu za Sala ni kama Safu za Malaika.
2-Ardhi Yote imejaaliwa kua ni Sehemu ya Kusali kwa ajili yetu.
3-Vumbi la Ardhi limejaaliwa kua ni Kitoharisho pale tutakapokosa Maji.*(Sahih Muslim)*

Naam..katika Hadith hii tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anawafahamisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhu* namna Waislam walivyofadhiliwa na kupendelewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika mambo matatu tofauti na Watu waliotangulia.

Ambapo Jambo la kwanza ni Kupanga Safu za Sala kama wapangavyo Malaika mbele ya Allah Subhanah wa Ta'ala kwani Malaika huanza Mstari wa mbele na kisha wakishaujaza ndio huanza Mstari wa pili yake. Kama ilivyosemwa katika Sunnah Abu Daud. '**Pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipowauliza Masahaba zake Jee Hamtaki Nyinyi kupanga Safu kama Malaika mbele ya Mola wao?**

Masahaba *Radhi Allahu Anhu* wakauliza: 'Kwani Malaika wanapanga Vipi Safu?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Wanakamilisha Safu ya kwanza kwanza na kukaribiana katika Kusimama katika Safu.'**

Jambo la pili ni kua Ardhi imejaaliwa kua ni sehemu ya Kusujudia kwa Waislam, kwani watu w Ummah zilizotangulia walikua wakiruhusiwa Kusali katika sehemu Maalum, kama kwenye Masinagogj, Makanisani, na kwenye Mihirabu tu.

Kama ilivyosemwa katika Musnad Imam Ahmad kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Wale waliotangukia Kabla yangu walikua wakisali kwenye Makanisa tu.'**

Na akasema tena *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Hakuna miongoni mwa Mitume ambao walikua wakisali katika sehemu yeyote ile Isipokua katika Mihirabu.'**

Na kuhusiana na jambo la tatu ambalo ni Kujaaliwa kwa Ardhi kua ni Toharisho kwa njia ya Tayammam, ambalo lililoruhusiwa kwa ajili ya Ummah wa Kiislam tu. Ambapo katika Hadith nyengine basi tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameainisha Jambo jengine ambalo Tulilofadhiliwa Waislam peke yetu kua ni Aya mbili za mwishoni mwa *Surat Al Baqara* yaani Amana Rasul ambazo ni hazina iliyokua chini ya Arshi ya Allah. Kama ilivyoelezewa na Imam Ibn Khuzaymah na Imam An Nasai.

Hivyo nasi tumeiangalia hadith hii kukumbushana kuhusiana na namna *Allah Subhanah wa Ta'ala* alivyotupendelea kifadhila kuhusiana na Tayammam.

Na kama tulivyoona kua kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wamesema kua Tayammam hua ni kwenye Mchanga Uliokua Msafi na Tohara kama alivyotufafanulia Imam Al Mawardi. Ambapo kwa upande mwengine basi anasema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua: '**Imam Malik na Imam Abu Hanifa wamesema kua Tayammam inakubalika kwa kila kitu kitokanacho na Mchanga, kama Udongo Tofali, Madini ya Ardhini, Jiwe n.k.**' *(Al Mughni)*

Na akasema Imam Al Shurunbulali Al Hanafi pia kua: '**Katika Madhhab yetu inakubalika kufanya Tayammam kwa kutumia kitu chochote kinachotokana na Ardhi Kimaumbile kama Mchanga na Mawe.**'*(Maraqi Al Falah)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Qarafi basi amesema kua: '**Kama Jiwe likisagwa na kisha Unga wakeuatumiwa kwa ajili ya Kutayammam basi Tayammam hio hu ani batili.**'*(Al Dhakiira)*

Naam..Miongoni mwa Masuali kuhusiana na Tayammam ni kua: **'Jee Kama Muislam amefariki katika Mazingira ya Ardhi ambayo haina Maji, kwa Mfano kama Jangwani, na Waislam wenzake hawana Maji ya Kumkoshea Au Maiti Ameungua Moto, au Maiti Amekaa Majini kwa mda mrefu na Ngozi Imelainika na kubanduka haiwezekani kumkosha afanyweje?**'

Ambapo kuhusiana na Suali hili basi Amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Kama ikiwa kuna dharurah au kisingizio kinachokubalika Kisharia cha kutowezekana kumkosha Maiti kwa Maji, kwa Mfano kwa sababu ya kutokana na Kukosekana kwa Maji au Labda Kuungua vibaya sana kwa Maiti kiasi ya kua kama akikoshwa Maiti husika basi Nyama yake itakua Inabanduka.**

Na kuachana na Mwili wake, basi katika hali kama hii kwa Maiti husika hua anastahiki Kutoharishwa kwa Njia ya kufanyiwa Tayammam. Na Tayammam hua ni Wajibu kwa Maiti mwenye kua katika mazingira kama haya kwa sababu hua ni miongoni mwa Njia za Kumtoharisha ingawa hua haihusiana na Kumtoa Uchafu.

Hivyo Hua ni Wajibu kutumia Njia ya Tayammam pale itakapokosekana Maji au itakapokua haiwezekani kwa Maji kama vile ilivyokua katika Kukoga Janaba.'*(Al Majmuu)*

Ambapo hapa kwanza inapidi ifuatwe njia ambayo kulingana na Mfumo wa Tahqiq Al Manath ambayo hua ni Njia ya Kujitahidi Kuchunguza na kufuatilia kwa ambayo itakua imetumika au imetajwa kwenye Maandiko, au Makubaliano ya Wanazuoni, au kutumia njia ya Istinbat pale itakapokua hakuna uthibitisho kwenye Maandiko.

Na hivyo basi ikiwa kumekosekana Uthibitisho wa katika kesi husika basi kitakachofuatiliwa hua ni kuangaliwa Kanuni za Fiqh zinasemaje. Ambapo miongoni mwa Kanuni za Fiqh imo ile inayosema kua:

البدل مكان المبْدَل إذا تعذر المبدل منه

'Al Badal Makan Al Mubaddal Idha Taidhr Al Mubdi Minhu **- Kitu Mbadala Huchukua Nafasi ya Kitu kinachobadilishwa kama ikiwa Kitu kinachobadilshwa Hakipatikani.'**

Na hivyo kutokana na kua Tayammam hua inachukua ya Badilisho La Udhu yanapokosekana Maji, basi katika hali na Mazingira kama haya basi Vumbi la Tayammam hua ni mbadala wa Maji na hivyo kutokana na Kua Maiti ya Kislam ni lazima ikoshwe kabla ya Kusaliwa na kuzikwa lakini kwa kua Maji ya kumkoshea yamekosekana basi Tayammam itachukua nafasi ya Josho.

Ambapo hapa sasa itabidi Mtu Husika atakaemfanyia Tayammam Maiti husika hua ni mwenye kutakiwa Kutia Nia na kisha Kupiga Mikono yake Kwenye Mchanga Safi na Tohara na kisha kumpangusisha Maiti husika Usoni na Mikononi mwake kisha kumvisha Sanda, na kumsalia na Kumzika.

Kwani amesema Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* kua:

عن عمرو بن العاص رضي الله عنه أنه لما بعثه الرسول صلى الله عليه وسلم في غزوة ذات السلاسل قال: احتلمت في ليلة باردة شديدة البرد فأشفقت إن اغتسلت أن أَهْلِكَ، فتيممت ثم صليت بأصحابي صلاة الصبح، فلما قدمنا على الرسول صلى الله عليه وسلم ذكرت ذلك له، فقال: " ياعمرو صليت بأصحابك وأنت جنب ؟ قلت: نعم يا رسول الله، إني احتلمت في ليلة باردة شديدة البرد، فأشفقت إن اغتسلت أن أهلك، وذكرت قول الله (ولا تقتلوا أنفسكم إن الله كان بكم رحيماً) فتيممت ثم صليت، فضحك رسول الله صلى الله عليه وسلم ولم يقل شيئاً"

Nilipotumwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Vita vya Dhatu Salasil, Ilikua kuna Usiku wenye Baridi kali sana. Na nilipolala Usiku na kuamka Alfajiri nikajikuta kua ni mwenye Kuamka na Janaba.

Na Kutokana na Baridi iliyopo basi nikawa na Uhakika kua kama nikikoga Siko hio Basi nitakua ni Mtu mwenye bahati mbaya sana. Hivyo Nikatayammam, na kisha Nikawasalisha Wenzangu Sala ya Alfajr. **Na tuliporudi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wenzangu wakamhadithia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya habari hio. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaniuliza kwa kusema: Ewe Amr! Umewasalisha wenzio wakati ukiwa katika hali ya Janaba?'**

Nami nikajibu kwa kusema: 'Ya Rasul Allah! Hakika mimi nilikumbuka Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema katika Qur'an kua: "Msijiangamize kwa Mikono yenu, kwani kwa Hakika Allah ni mwingi wa Huruma juu yenu" hivyo nilifanya Tayammam na nikasali. **Baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusikia Jibu hilo basi akacheka na kisha hakusema chochote.'** *(Sunnan Abu Daud, Mustadrak Al Hakim)*

Naam..kabla ya kuendelea basi tukumbushane kua Amr Ibn Al Aas *Radh Allahu Anhu* ni Sahaba ambae alikua ni mwenye kua na Sifa ya kua ni Mtu mahiri sana wa Lugha ya Kiarabu, mwingi wa hikma, mwingi wa hoja na ni mwingi wa Ufahamu wa mbinu za Vita.

Ingawa hamkutii Khalid Ibn Walid *Radhi Allahu Anhu*, lakini kwa upande wake Amr Ibn Al Aas ambae alisilimu siku moja na Khalid Ibn Walid Radhi Allahu Anhum na baada ya kusilimu kwao basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwaambia Masahaba wake Mjini Madina kua: '**Mji wa Makkah umekutupieni Vipande vya Moyo wake.'**

Hii ni kutokana na Umuhimu wao kwa Uislam katika wakati huo. Na tunapomzungumzia Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* kabla ya kusilimu kwake basi tunaona kua Makafiri wa Makkah walikua wakimtumia Sana Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* katika Majadiliano ya Kihoja mbali ya kua na umri mdogo.

Na ndio maana Makafiri hao wakamteua Amr Ibn Al Aas kuenda Habashi kwa kujadiliana na Mfalme Najash ili awafukuze Waislam waliokimbilia huko wakiongozwa na Jafar Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu.*

Na baada ya kusilimu kwake siku Moja baada ya kufariki *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi Amr Ibn Al Aas aliulizwa na Abu Bakr Al Siddiq *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema: '**Ewe Amr! Hakika wewe ndie mwenye Busara zaidi miongoni mwa watu, nami nataka kumuachia Khalid Ibn Walid Uongozi wa Jeshi la Kiislam kama alivyofanya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Jee Unasemaje Juu yake?.'**

Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* akasema: **'Ewe Abu Bakr! Hakuna Mtu mwenye Sifa stahiki ya kubeba wadhifa huo kama Khalid Ibn Walid, kwani Khalid ni Kiongozi mwenye Subira ya Paka, Mtizamo wa Macho wa Kipanga na Mvamio wa Mapigano wa Simba.'**

Naam..kwa leo tusimamie hapa huku tukitaariifiana ni kwa Nini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alicheka namna Amr Ibn Al Aas alivyojibu Suali aliloulizwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa Hoja na Vithibitisho vya Aya. Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akijua kua Amr Ibn Al Aas *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hatokosa kisingizio cha Kujitetea, kwanini akawasalisha watu huku akiwa na Janaba. Na bila ya shaka kisingizio chake kinakubalika hususan baada ya kuegemea zaidi kwenye Aya.

Kwani kama tulivyosema hapo awali kua Hukumu ya Tayammam basi hua haitoharishi, bali hua inampelekea Mtu Kuruhusika kuingia kwenye Ibada pale atakapokua na Dharurah ya Kukosa Maji, Kua anaumwa au kua katika Mazingira hatarishi ya Maisha yake kama akitumia Maji ka.a tutakavyofafanua zaidi juu ya Hadith hii ambayo tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameonesha hali ya Takrir yaani hali ya kukubaliana na kile anachoambiwa na hivyo kukaa kimya bila kupinga.

Hivyo amesema Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* kua: Nilipotumwa *na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Vita vya Dhatu Salasil, Ilikua kuna Usiku wenye Baridi kali sana. Na nilipolala Usiku na kuamka Alfajiri nikajikuta kua ni mwenye Kuamka na Janaba. Na Kutokana na Baridi iliyopo basi nikawa na Uhakika kua kama nikikoga Siko hio Basi nitakua ni Mtu mwenye bahati mbaya sana. Hivyo Nikatayammam, na kisha Nikawasalisha Wenzangu Sala ya Alfajr

Na tuliporudi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wenzangu wakamhadithia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya habari hio. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaniuliza kwa kusema**: 'Ewe Amr! Umewasalisha wenzio wakati ukiwa katika hali ya Janaba**?

Nami nikajibu kwa kusema: '***Ya Rasul Allah!* Hakika mimi nilikumbuka Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema katika Qur'an kua: 'Msijiangamize kwa Mikono yenu, kwani kwa Hakika Allah ni mwingi wa Huruma juu yenu" hivyo nilifanya Tayammam na nikasali.'**

Baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusikia Jibu hilo basi akacheka na kisha hakusema chochote.'*(Sunnan Abu Daud, Mustadrak Al Hakim)*

Naam..hivyo kutokana na Hadith hii ua Amr Ibn Al Aas Radhi Allahu Anhu basi tunaona kua Wanazuoni wanasema kua: '**Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hua ni Wajibu kwa Maamuma alietia Udhu kumfuata Imam Aliefanya Tayammam lakini kwa sharti la kua kama Imam husika atakua na Wajibu wa kuirudia Sala hio hapo baadae atakapopata Maji, kwani kama ikiwa hatokua na Wajibu wa Kuirudia Sala hio basi hua haikibaliki kumfuata Imam huyo.'**

Ambapo ili kufahamiana zaidi basi na tumuangalie Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi ambae anatuambia kua**: 'Inakubalika kwa Mtu alietia Udhu Kumfuata Imam ambae amepaka Maji kwenye Khuf (Soksi za Ngozi) na pia kwa Mtu alietia Udhu kusali Nyuma ya Imam aliefanya Tayammam lakini pale itakapokua Imam husika hatowajibika Kuirudia Sala yake hio. Yaani kama katika hali ya Imam ambae anafanya Tayammam kwa sababu ya kua amekoaa Maji na yuko Safarini, au ni Tayammam ya Mtu ambae yuko Nyumbani lakini Anaumwa, au ana Jeraha n.k na haya ndio makubaliano ya Wanazuoni wa Skuli ya Madhhab yetu.'**(*Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na pia amesema Shaykh Ul Islami Imam Ahaihab Ad Din Al Ramli kua: '**Hairuhusiki kwa Mtu kumfuata Imam ambae amefanya Tayammam na kisha akawa anawajibu wa kuirudia Sala husika, kama vile kwa mfano Sala ya Faqidh Al Tahurayn yaani Mtu ambae amezuilika kutumia Maji au Mchanga au Mtu ambae anafanya Tayammam kwa sababu ya Baridi au kwa sababu ya kukosa Maji.'**(*Fath Al Rahmam Sharh Zubad Ibn Ruslan)*

Ambapo Imam Ali Shabramilisi Al Shafii akafafanua kuhusiana na hoja ya Uthibitisho wa Hadith yetu hii ya Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema kua: '**Ama Kuhusiana na Hadith hii basi tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumlazimisha Amr Ibn Al Aas na Masahaba wenzake *Radhi Allahu Anhum* kurudia Sala zao kwa sababu hii imejumuishwa kwenye Taakhir Al Bayyan ila Waqt Al Hajjah yaani Kucheleweshа Ubainifu wa Kitu hadi pale utakapowadia mda Stahiki, na hivyo hii hua inaruhusika, na pia inawezekana ikawa pia Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* alikua anajua kua katika Hali aliyokua nayo basi alikua anatakiwa airudie Sala yake hio.**

Ama kuhusiana na Masahaba wenzake *Radhi Allahu Anhum* aliowasalisha basi inawezekana kua katika Wakati ambao walikua wakisalishwa basi hawakua wakijuakua Imam wao alikua katika haki aliyokua nayo*.'(Nihayat Al Muhtaj na pia ndivyo Alivyosema Al Khatib Al Shirbini katika Al Mughni Al Muhtaj)*

Hivyo basi kuhusian na Suali hili tunahitimisha kwa kusema kua:

1-Hukmu ya Kumfuata Imam aliefanya Tayammam ambae itambidi airudie Sala yake hio basi Sala hio hua ni Batili kwani hua haikubalikii kumfuata na akimfuata basi itambidi airudie Sala hio.

Na mifano juu ya hili ni kama asemavyo Imam Al Khatib Al Sbirbini kua: Tayammam inayokubalika ni ya Yule Mtu ambae anaishi katika Sehemu ambayo kimaumbile hua haina Maji kama Jangwani.

Hivyo kama ikiwa Mtu anaishi katika Maeneo kama haya basi Tayammam yake inakubalika na haitombidi Mtu huyo kuirudia Sala hio, lakini kama itakua ni kwa Mda mfupi tu basi itambidi kurudia Sala.

Mtu ambae anaefanya Tayammam kwa sababu ya Mazingira ya Hali ya Hewa ni Baridi sana na hivyo hawezi kutumia Maji kwani yatamdhuru na hakuna njia ya kuyapasha moto, na hii ni kutokana na kua Hali hii hua ni mda mfupi tu basi, basi itambidi airudie Sala yake akipata Maji.'*(Al Mughni Al Muhtaj)*

2-Hukmu ya Kumfuata Imam anaefanya Tayammam na akawa haitakiwi kwake kuirudia Sala hio hata baada ya kuona Maji,hua inakubalika kumfuata na Sala i nakua Sahih na hatowajibika Maamuma Kuirudia Sala hio.

Mfano wa hali hizi kama: Mtu ambae anafanya Tayammam kwa sababu ya kukosa Maji na yeye yuko Safarini katika Safari ya Kihalali na wala si Safari ya kwa ajili ya kufanya Dhambi.

Mtu anaefanya Tayammam kutokana na Maradhi au Jeraha na akitia Udhu atahatarisha ḳupona kwake iwe ni msafiri ama la. *(Al Mughni Al Muhtaj)*

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah An Nawawi Al Shafii katika Kitabu chake cha Al Majmuu kua: '**Masharti ya kuruhusika kwa Tayammam ni Manne:**

1-Mtu anaetaka Kufanya Tayammam awe ni lazima mwenye Kuruhusika kujitoharisha kama tulivyosema hapo awali kuhusiana na Udhu.

Yaani Sifa za Mtu mwenye Kuruhusika Kujitoharisha kwa Udhu awe ni Muislam Na asiwe na Najis ya kitu chochote kinachobatilisha Udhu kama tulivyoelezea hapo kabla juu ya Mkojo, Kinyesi, Madhii, Madii, Hedhi, n.k.

2-Lazima awe ni mwenye Kuupata Mchanga Msafi na Tohara kwa ajili ya Kutayammam.

3-Mtu anaetaka Kufanya Tayammam awe ni mwenye Dharurah inayomruhusu Kisharia kufanya Tayammam kama kukosa Maji,au kutokua na Uwezo wa Kutumia Maji, kama tutakavyoelezea hapo baadae.

4-Mwenye Kutaka Kufanya Tayammam anatakiwa afanye tu Mara baada ya Wakati wa Sala husika kua Umeshaingia, kwa Sababu Vitabu vya Imam Al Shafii na Wanafunzi wake Wanakubaliana kua Tayammam kwa ajili ya Sala ya Fardhi hua haikubalikia hadi pale utakapoingia Wakati wa Sala husika.

Na hii hua kwa kila aina ya Dharurah inauokubalika kufanya Tayammam kama Kukosa Maji, Kutoweza kutumia Maji, Kua na Jeraha lisilotakiwa Kutiwa Maji,Kuumwa n.k.'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kutuambia kuhusiana na Sharti la Wakati wa Tayammam kwa kusema kua: '**Qadhi Abu Tayyib katika Sharh yake amenukuu Ijmaa au Makubaliano ya Wanzuoni juu ya kukubalika kwa Tayammam ya Mtu ambae ametayammam kwa ajili ya Sala ya Fardhi na kisha akakumbuka kua kumbe kuna Sala nyengine.**

Ambapo hii inatuthibitishia kua kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu kua Tayammam iliyonuiwa kwa Sala ya Fardhi hua ni kwa ajili ya Sala ya Fardhi husika tu. Ama kuhusiana na Tayammam ya Sala ya Sunna basi hua kuna aina mbili kuna ya Muda mdupi na nyenginezo, ambapo kuhusiana na nyenginezo basi Mtu anaruhusika kutayamm katika Mda autakao isipokua

kwenye Mda ambao imekatazwa kusali ndani yake, ambapo Mtu hua hatakiwi pia kifanya Tayammam ndani yake Ya Fardhi ambayo bado hajaisali.

Ambapo kwa upande wa Imam Al Qaffal Al Shashi Al Marwazi basi amesema kua: Wanazuoni wanakubaliana kua Inakubalika Kusali Sala ya Kabla aliyoikimbuka kabla ya Kusali Kadhaa ya pili kwa Tayammam ya kwanza.Na kwa upande wa Imam Al Baghawi basi yeye anasema kua Inakubalika kufanya hivyo kulingana na Mtizamo wa Juu juu wa Madhhab lakini kwa mtizamo mwengine basi hua haikubaliki.

Ambapo kwa Upande wa Al Al Shafii basi amesema kupitia kwa Imam Al Buwayti kua Kama ikiwa Mtu atafanya Tayammam katika Wakati usioruhusika kusali basi Tayammam yake hio itakua Batili, na hata kama akisali baada ya kupita mda uliokatazwa kusali kwa Tayammam hio basi Sala yake hua ni Batili kwa sababu kua amefanya Tayamma kabla ya wakati wa Sala. Ambapo kwa Qadhi Al Husayn na Imam Al Mutawali basi wao wamesema kua: 'Kuna Mtizamo miwili kuhusiana na Kukubalika kwa Tayammam ya Mtu aliefanya Tayammam katika wakati uliokatazwa kusali kama ikiwa Sala hio ilifanywa ndani ya Wakati huo.

Ambapo Imam Al Ruwayni na Imam Al Qaffal Al Shashi Al Marwazi wanasema kua Kama Mtu atafanya Tayammam kabla ya Mda usiotakiwa kusali,na kisha akasali baada ya Mda huo basi Tayammam yake hua haikubatilika, na hakuna kutofautiana juu ya hilo.

Ama kuhusiana na Tayammam ya Sala ya ndani ya Mda mfupi basi Tayammam hainaSharti kama ilivyosemaa kwenye Tanbih.

Hivyo Wanazuoni wa Khurasan wanakubaliana kua Tayammam ha haikubaliki isipokua pale utakapoingia Wakati wa Sala. Na Imam Al Rafii amesema kua huu ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii. Na Imam Al Haramayn na Imam Al Ghazali wamenukuu Mitizamo miwili pia ambapo mmoja ndio huu na wa pili ni kua:

'Inaruhusika kufanya Tayammam kabla ya kuingia wakati wa Sala kutokana na kua wakati wa Sala hua si kwa ajili Ya Sala za Fardhi tu, hivyo Tayammam moja kwa ajili ya Sala za Sunnah hua inakubalika kwa Sala nyenginezo za Sunna. Kwani Nyakati za Sala za sunna kama Witr, Dhuha, Idd n.k hua zinajulikana kulingana na nyakati za meneo husika.

Ambapo wakati wa Sala ya Kupatwa kwa Jua au Mwezi hua ni pale kinapopatwa kitu husika, wakati wa Sala ya Mvua Istiqsa hua pale watu wnapokusanyika Sehemu kwa ajili yake, na wakati wa Sala ya Kuamkia Msikiti hua pale unapoingia Msikitini, hivyo basi hapa kuna hoja nyingi kuhusiana na Sala za Sunnah, hivyo Kauli ya Imam Al Ghazali inasisitiza kua hukumu hio hua ni kwa ajili ya Sala za Fardhi tu, wa Allahu Aalam.

Ama kuhusiana na Tayammam ya Maiti basi hua ina Mitizamo miwili juu yake. Ambapo Mtizamo unaokubalika zaidi ni kua hua inajumuishika katika wakati wa Kumfayia Tayamma Maiti kwa sababu ndio wakati wake na inatosheleza. Na hivyo ndivyo alivyosema Imam Al Haramayn, Imam Al Ghazali katika vitabu vyake na Imam Al Baghawi pia.

Ambapo Mtizamo wa Pili ni hua inategemea na kifo chenyewe kwa sababu aina ya kifo ndio inapelekea kufanywa kwa Tayammam, na Imam Al Ghazali amethibitisha hayo katika Fatwa zake na Imam Al Shashi Al Qaffal amethibitisha pia.

Ama kwa upande wa Qadhi Al Husayn basi yeye amesema kua Tayammam ya Maiti hua inapendekezwa kufanywa baada ya Kumvisha Sanda na hii ni kwa sababu hua haipendekezwi kumsalia kabla ya Kumvisha Sanda hata kama ikiwa inaruhusika.

Hivyo kama ikiwa Mtu atakosa Maji ya Kumkosha Maiti, basi anatakiwa Amfanyie Tayamam ya Kumtoharisha kwanza na kisha Tayammam ya kumsalia, na bila ya shaka Tayammam ya Mfanyishaji Tayammam mtu mwengine hua haikubaliki hadi huyo mfanyaji awe nae ameshatayammam, w Allahu Aalam*(Al Majmuu Sbarh Al Muhadhhab)*

Na baada ya Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kuelezea mitizamo ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana kuruhusika kwa Tayammam moja kwa kila Sala ya Fardhi na ulazima wa Kutayammam katika wakati unapoingia mda wa Sala husika basi anarudi katika Kutetea msimamo kwa kusema kua:

Kama tulivyosema kua Tayammam kwa Ajili ya Sala Ya Fardhi hua hairuhusiki hadi pale utakapoingia Mda wa Sala husika, ambao ndio Mtizamo wa Madhhab yetu na Madhhab ya Imam Malik, Imam Ahmad na Daud na wengi miongoni mwa Wanazuoni.

Ambapo kwa upande wa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: 'Tayammam ya Sala ya Fardhi hua inakubalika hata kama haujaingia wakati wa Sala husika.'

Kutokana na kua wao wanasimamia Hoja yao kwa kulinganisha Tayammam na Udhu na kupangusa juu ya Soksi za ngozi Na kujitoharisha kutokana na Najis. Kwa sababu wanachukulia kua katika hali hii Tayammam hua inafanywa pale inapostahiki kua kama ni mbadala wa Udhu.

Lakini Wanazuoni wetu wanasimamia kwenye maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema katika aya za Udhu na Tayamma kua:

﴿ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيداً طَيِّباً ﴾

falam tajidoo maaa'an fatayammamoo sa'eedan taiyiban *(Surat Al Maidah 5:6)*

Tafsir: **Hivyo Kama Hamkupata Maji Basi Fanyeni Tayammam kwa Mchanga Uliosafi na Mzuri***(Surat An Nisaa 4:43, Al Maidah 5:6)*

Ambapo Aya hizi hua zinamtaka Mtu husika ambae tayari amesimama anataka Kusali, na hivyo ruhusa ya Kutia Udhu kabla ya wakati haikujumuishwa kwenye vitendo vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam na* Makubaliano ya Wanazuoni.

Hivyo kama Tayammam ikiwa inafanywa bila ya Kutakikana, hua ni batili, kama vile ambavyo Mtu anaefanya Tayammam huku akiwa na Maji.

Na kama wakisema kua kama ni hivyo basi Tayammam itatakikana kufanywa mwishoni mwa Kipindi cha Sala, basi aiai tunasema kua Mtu hua anatakiwa kujiondolea Jukumu La Sala ndani ya Wakati wake kwa Kuifanya Mwanzoni mwa wake wake.

Kwa sababu Tayammam hua ni Toharisho la Dharurah kama vile ilivyokua kaa Mwanammke mwenye Damu ya Istihadhah, ambapo wao Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wanakubaliana na hili.

Kwani amesema Imam Al Haramayn katika Al Asalib kua: Kuruhusika kwa Tayammam baada ya kuingia wakati wa Sala kumethibitishwa Tofauti na Tayammam ambayo hufanyaa kutokana na Dharurah na hivyo hua imo ndani ya Mipaka ya Mazingira ya Dharurah husika, kama vile inavyoruhusika kula Mzoga.

Hivyo Tayammam hua inakubalika kwa ajili ya kuruhusika Kufanyika kwa Ibada ya Sala, ambapo hata hivyo Sala kabla ya kuingia wakato wake hua haikubaliki.

Ama tunapozungumzia kuhusiana na hoja ya kufananisha na Kupangusa Khuff -Soksi za Ngozi laini- basi sisi tunasema kua hio hua ni kukubaliana Na kua na Uvivu, hivyo hua hakuna mipaka ya wakati juu yake.

Kwani Kupangusa Khuff hua kunaruhusika wakati Mtu akiwa na uwezo wa Kuikosha Miguu yake, wakati Tayammam hua ni Dharurah, na hivyo hua haikubaliki pale Mtu atakapokua na uwezo wa Kutumia Maji.

Ama kuhusiana na Hoja yao kua Tayammam inakubalika hata kabla ya wakati Inakubalika kwa sababu Tayammam hua ni Mbadala wa Udhu.

Basi hii hua ni sawa na namna inavyobatilika kile ambacho kinabatilika wakati wa Usiku, ambacho usipokifanya mchana hubidi kulipia kafara yake lakini hua si mbadala wake yaani Funga ambayo mchana wake hua unabatilika katika Siku ya Idd.

Na amesema Imam Ad Darimi kua amesema Abu Said Al Istakhri kua, 'Hakika sisi hatuwezi kuhojiana na kulumbana na Wanazuoni wa Hanafi juu ya hili kwa sababu tayari wameshakiuka Makubaliano juu yake, w Allahu Aalam.'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Hivyo baada ya kuangalia kuhusiana na Hukmu na Masharti ya Tayammam kulingana na Mitizamo ya Qadhi Al Qudhat Imam Al Mawardi Al Shafii na Shaykh Ul Islami Imam An Nawawi Al Shafii na Maimamu wa Madhhab mengineyo basi tuhitimishe kwa kuelezea jumuisho fupi kuhusiana na Tayammam na hivyo ndani yake tunaona kua:

'Tayammam hua ni njia ya Kutumia Mchanga Safi na Tohara Kwa kupiga viganja Vya Mikono juu ya Mchanga husika na kisha Kukunuta Viganja hivyo na kisha kujipangusia Usoni Vumbi vumbi lililobakia viganjani na kisha kupiga mara ya pili na kujipangusia Kwenye Mkono wa Kulia hadi kwenye Kisugudi na kisha Mkono wa kushoto hadi kwenye Kisugudi kwa nia ya Kujitoa katika hali ya kutoruhusika Kusali na kuingia katika hali ya Kuruhusika kusali,au kujitoa kwenye Hali ya Janaba baada ya kukosa Maji ya Kujitoharishia.'

Hivyo basi Mtu anaetaka kufanya Tayammam kutokana na Kuruhusika Kisharia baada ya kukosa Maji kutokana na Sababu tofauti kama tutakavyoelezea hua na Ulazima baada ya kupata Mchanga stahiki hua ni mwenye Kutakiwa kuelekea Kibla kisha kusema Bismi Allahi Rahmani Rahim na kisha Kutia Nia kwa mfano Salat Dhuhr kwa kusema:

Nawaytu Istibahat Fardhi Salat Adh Dhuhr **- Nanuia Kuruhusika kusali Fardhi ya Adhuhuri**

Na kisha Kupiga Viganja vya Mikono Mchangani Huku Vidole vikiwa vimetawanyika na kisha Kukunuta Viganja hivyo kabla Kujipangusia vumbi vumbi lililobakia viganjani kwenye Uso Kama unavyojipangusia Maji kwenye Udhu wa Sala kwa kuanzia Juu Usoni kabla ya chini na kuanzia upande wa Kulia kabla ya kushoto.

Kisha kupiga Tena Viganja Mchangani kama mwanzo lakini badala ya kujipangusia Usoni basi unajipangusia Kwenye Mkono wa Kulia kabla ya Kushoto kwa kuanzia vidoleni kupanda juu kwa upande wa nje wa Mkono kuelekea Kisugudini na kurudi kwenye Vidole kupitia kwa upande wa Ndani wa Mkono na kuhakikisha kua sehemu yote ya Kiganja hadi Kisugudini umeguswa na vumbi vumbi la mchanga husika.

Hivyo kama umevaa pete au saa basi itabidi uvue kabla ya Tayammam, na kiaha utamalizia mkono wa kushoto kama ulivyofanya kwenye mkono wa kulia.

Na hutakiwi kusita kutoka katika hatua moja kuingia nyengine, kwa mfano Kupangusa Uso kisha ukavua pete labda au saa na kisha Ndio ukaanza mikononi, kwani kufanya hivyo kunabatilisha Tayammam yako na hivyo itabidi uanze tena Upya Tayammam hio.

Na kisha baada ya hapo utaomba Dua ya kuomba kukubaliwa Tayammam yako na kutia Nia ya Sala yako na kuingia ndani ya Ibada ya Sala yako, na unaruhusika Kuadhini na Kukimu pia kabla yake.

Kwani kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi Wao wanakubaliana kua: **'Tayammam kabla ya Wakati wa Sala ya Fardhi hua haikubaliki hivyo kuna Ulazima wa kua Wakati wa Sala husika ya Fardhi uwe umeshawadia**

Ambapo kwa Upande wa Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi kwao wao ni kua hakuna Ulazima wa Kuwadia kwa Wakati wa Sala husika, kwani unaweza kutayammam hata kabla ya kuingia wakati wa Sala Husika.'

Baada ya kuangalia Hatua za namna ya kufanya Tayammam basi tunaona kua miongoni mwa Mambo yanayompelekea Mtu kuruhusika kufanya Tayammam ambayo ni pamoja na:

1-Kukosekana kwa Maji Safi ya Kujitoharishia au kutilia Udhu si tu baada ya kua Mtu hana Maji bali pia baada ya kuyatafuta na kukosa katika mazingira ya sehemu aliyokuwepo.

2-Kua na hali ambayo Mtu husika amezuilika kutumia Maji kutokana na Maradhi, Jeraha au Baridi Kali sana kiasi ya kua kama Mtu atatumia Maji ambayo yapo na yanapatikana basi atahatarisha Uhai wake au Afya yake kwa kujizidishia maradhi husika n.k.

3-Kua katika hali ya mazingira ambayo maji yapo lakini hayawezi kupatikana kutokana na hali hatarishi ya kuyapata Maji hayo, kwa mfano labda karibu yake kuna Maadui ambao: Wanaweza kumuua mhusika au kumdhuru vibaya sana, aukuna Wadudu au Wanyama hatari kwa maisha ya Ibn Adam.

4-Kua na hali ya kua chini ya Ulinzi wa Maadui zako ambao hawakuruhusu kutumia Maji,au labda Kifungoni Jela ambamo haiwezekani kupata Maji. Ambapo kwa Mtu aliekua Kifungoni basi tumesema kua kama Hhamna mchanga basi anaruhusika kupangusa kwenye Ukuta kama Itakua una Vumbi vumbi na kutumia kwa ajili ya Tayammam, ambapo hii ni kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Na ingawa kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Hanbal hawaruhusu hivyo lakini kama ikiwa mtu hana njia nyengine basi anaweza kufuata Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik au Abu Hanifa katika hili.

Ambapo wao Wafuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik wanaruhusu kutumia pia Ukuta wenye Plasta ya Saruji na Rangi lakini isiwe rangi ya Mafuta au Kartasi ya kubandika Ukutani, Inaruhusika pia Vyombo vya Udongo na Kauri kama Vyungu, Mitungi, Mikungu, Sahani na Vikombe ila visiwe vinavyong'ara.

5-Kua na hali ya Kua Safarini au sehemu yeyote ile katika Mazingira ambayo Mtu hana Maji isipokua amebakiwa nayo kidogo sana ambayo ni kwa ajili ya Kunywa, na hakuna uwezo wa kupatikana Maji mengine.

Na Miongoni mwa Masharti ni kua kama tulivyosema kua Tayammam Moja hua kwa kitu kimoja ambacho ni kulingana na Nia yako. Yaani kama Ukitia Nia ya Tayammam kwa ajili ya kuondoa Janaba basi hutoruhusika Kusali na Tayammam hio hadi utie nia ya Tayammam ya Kuruhusika Kusali.

Hivyo Ukitia Tayammam kwa nia ya Sala ya Fardhi basi Utaruhusika kusali Sala ya Fardhi husika na Sunna zake, yaani kama Ni Salat Dhuhr basi ni Salat Dhuhr na Sunna zake tu. Hivyo ukitaka kusali Salat Al Asr basi utatia Tayammam nyengine hata kama ni Mda mfupi tu kupita baina ya Sala 2 hizo za Fardhi.

Na ukitia Nia ya Kuruhusika Kusali Sunnah basi Unaweza kusali Sunna hata 100 lakini kamwe hutoruhusika kusali Sala ya Fardhi kutokana na Tayammam ya Sunnat Salat.

Haikubaliki kufanya Tayammam kwa Kutumia Kigae, Kioo, Chuma, Plastiki, aina zote za Madini ya Ardhini, Kijiti, Ubao au Majani.

Watu Kadhaa wanaruhusika Kufanya Tayammam kutokana na Mchanga Msafi na Tohara wa sehemu moja hio hio bila ya Mchanga huo kua Mustaamal yaani Ambao umeshatumika hapo kabla kwa ajili ya Tayammam na hivyo kua haufai kutumika kwa ajili ya Mtu mwengine.

Na bila ya shaka kuhusiana na Yanayobatilisha Udhu hubatilisha pia Tayammam, ikiwemo pia Mtu kupata au Kuona Maji baada ya Kutayammam ambapo tukio hilo humbatilishia Tayammam yake.

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- DAMAN MASFUUHAN

❖❖❖❖

Tunaporudi kwa Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Sharaf An Nawawi Al Shafii basi tunaona kua anaendelea kutuambia kua: '**Mtizamo wa Madhhab yetu kuhusiana na Hadath ni Kua Hakuna Kitakachotoka Nje ya Mwili kitakachokua ni chenye kubatilisha Sala, isipokua pale kitu hicho kitakapokua kimetokea kwa kupitia Njia ya mbele na ya Nyuma za Haja.'***(Al Majmuu)*

Na tunapoaingalia Fatwa hii basi tunaona kua ni yenye kutokana na Kile kisa cha Masahaba wawili ndugu ambao ni Abbad Ibn Bishr ni Ansari na Amar Ibn Yassir ambae ni Muhajiri *Radhi Allahu Anhum.*

Ambapo Udugu wao Ulianzia pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipowaambia Masahaba zake wa Madina kua Kila Mmoja achague Sahaba mmoja kutoka Makkah ili awe ni ndugu yake.Hivyo Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* akamchagua Amar Ibn Yasir R*adhi Allahu Anhu.*

Naam..kisa kilichotoa Fatwa hii tunayoizungumzia kinaanzia miaka minne ya baada ya Mwaka Al Hijr.

Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipopata habari kua Makafiri wa Najd wanajitayarisha Kuvamia Mji wa Madina.Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakusanya Jeshi kuelekea Mashariki ya Mji wa Madina kwa ajili ya Kukabiliana na Jeshi la Maadui kabla halijakaribia katika Mji wa Madina.Huku akimuachia Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* Usimamizi wa Mji wa Madina.

Na miongoni mwa waliokuwemo kwenye Msafara wa Jeshi hilo alikuwemo pia Abbad Ibn Bishr na Ammar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu.*Ambapo Msafara ulipowadia katika maeneo ya Najd basi akakuta Mji huo ukiwa na Wanawake tu, kwani Wanaume wote wamekimbilia Milimani kujipanga Kimapigano.

Na hivyo ulipowadia wakati wa Salat Al Asr basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasalisha Sala ya Khofu ya Vita, kwa Nusu ya Waislam kusali na Nusu Kusimamia Ulinzi, na kisha Kubadilishana kaa Wanaolinda Kusali na Waliosali kulinda.

Tukio hili liliwapelekea wapiganaji wa Najd walioijificha Milimani kuona Wingi na Msimamo wa Waislam na hivyo kuamua Kutoshuka Milimani. Hivyo Baada ya Kuona Kimya Basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaona kua Imetosha kuonekana kwao na hakuna haja ya kupigana na Maadui zao kwani kama wangetaka basi wangewafuata kupigana nao. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamua kuondoa Jeshi na kurudi katika Mji wa Madina kwa salama na amani.

Msafara ulipotoka Nje ya Mji na kuingia kwenye eneo la bonde na Tambarare basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akachagua eneo na akaamrisha kupiga kambi katika eneo hilo. Na kisha akauliza : '**Jee ni Nani na Nani watasimamia ulimzi wa Usiku wa Leo?'**

Ambapo Abbad ibn Bishr na Ammar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhum* wakasema: '**Jukumu hilo litakua letu sisi Ya *Rasul Allah*!'**

Baada ya kupiga Kambi na Usiku kuingia basi basi Abbad Ibn Bishr akamuuliza Ammar Ibn Yasir kwa kusema: '**Ewe Ndugu yangu Jee Unataka Kulinda sehemu gani ya Usiku? Ya Mwanzo au ya Pili?.'**

Ambapo Ammar Ibn Yasir akajibu**: 'Wacha Mimi niupunguze Usingizi kwanza hivyo nitalinda sehemu ya pili.'** Na kisha akalala.

Hivyo baada ya Waislam kulala basi Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* akaabakia macho huku akiangalia huku na kule. Akavutiwa na madhari ya bonde Ambalo usiku wake ulikua tulivu sana huku Mbingu zikiwa zimepambinga vizuri na Nyiote zake ambazo kwa mbali zikionekana kama kwamba zimegusana na vivuli vya Miti na Majabali yaliyokua yametulia.

Hivyo Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* akaona kua hakuna mda mzuri kwake wa kuutumia kwa Ibada ya kumtukuza Mola wake kama Usiku huo. Na aakatia Udhu akaelekea Kibla na kisha akaingia kwenye Ibada ya Qiyam Al Layl.

Akasoma Surat Al Fatiha na kisha akaikamata Surat Al Kahf na kuanza kutirirka nayo kwa sauti yenye kuvutia na Ufahamu yakinifu juu ya yaliyomo ndani ya kila ujumbe wa Aya ambazo ndani hake zinazungumzia kuhusiana na Utukufu wa Imani, Haki, Subra na Uhusiano wa Kiwakati kulingana na visa vilivyomo ndani yake na mafunzo yake.

Wakati Abbad Ibn Bishr akiwa amezama ndani ya Utamu wa Ladha ya Kisomo cha Qur'an na Ladha halisi ya Ibada ya Sala.Basi kwa mbali mmoja kati ya Watu wa Najd akamuona Abbad Ibn Bishr Radhi

Allahu Anhu na hivyo akaona kua wacha ajaribu bahati yake na hivyo akachomoa Upinde wake na kupachika Mshale wa Upinde na kumtunga shababa Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu,* na kisha akauachia Upinde huo.

Ghafla Upinde huo ukazama kwenye Nyama ya mkono wa Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu,* ambae nae hakuweza kuhisi maumivu ya Mshale wa upinde huo kutokana na Utamu wa Ladha ya Surat Al Kahf na Sala yake. Bali aliukamata mshale huo Na kuutoa kwenye Mwilo wake na kuendelea na Sala yake huku Damu zikiwa zinamtoka. Sekunde chache baadae Ukafuata Upinde mwengine kwenye mwili wake na kisha ukafuata mwengine pia.

Radhi Allahu Anhu, akaitoa Mipinde hio mmoja baada ya mmoja huku akiendelea na Kisomo chake kirefu, kutokana na kua Surat Al Kahf ni yenye kua na Aya 110. Na kisha akarukuu, na kisha akanyanyuka na kusjudu Sijda ya kwanza, akasjudu ya Sijda ya pili lakini alipotaka Kunyanyuka akashindwa hivyo akamuamsha Ammar Ibn Yasir*Radhi Allahu Anhu* kwa kumwambia: '**Amka uendelee kulinda kwani kwa hakika mimi siwezi kuendelea kwani nimeshajeruhiwa.'**

Ammar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* akashtuka na kuanza kupiga Kelele kuwatahadharisha Waislam na kisha akamuuliza Abbad Ibn Bishr kwa kusema: '**Subhanah Allah Ilikuaje? Kwanini hukuniamsha wakati ulipopigaa Upinde wa Mwanzo tu?.'**

Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* akajibu: '**Kwa sababu nilikua niko katikati ya Kisomo cha Aya za Qur'an ambazo zilikua zinapa Utamu ndani ya Roho yangu na hivyo sikutaka Kukikatisha Kisomo kwani pia Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam aliniamrisha mimi kuihifadhi Sura hii, hivyo kwangu mimi Kifo ni bora kuliko kukatisha kisomo cha Sura Al Kahf..'**

Naam..hivyo mbali ya Kua *Rasul Allah Salallahu* Alayhi wa Salam hakumkataza Abbad Ibn Bishr Radhi Allahu Anhu wala hakusema kua Sala yake ni Batil lakini katika Hadith hii ambayo inapatikana katika vitabu vya Tarikh na pia katika Sahih Al Bukhari, Sunnan Abu Daud na Sahih Imam Ibn Khuzaymah tunaona kua Hadith hii ina mafunzo mengi sana kwa wenye kutafakkar.

Hivyo baada ya kuangalia Mfano wa Hadith ya Abbad Ibn Bishr Radhi Allahu Anhu ambae alikua Akisali huku akiwa anatokwa na Damu baada ya Kushambuliwa na Upinde katika Sehemu tatu tofauti za Mwili wake. Basi tunarudi kwa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi ambae anatuambiia kuhusiana na Kisa hicho kua:

'Abbad Ibn Bishr alikua akiendelea Kusali mbali ya Kua ni mwenye kutokwa na Damu, na hivyo kutokwa na Damu kwake hakukumbatilishia Udhu wake. **Na bila ya Shaka Rukuu na Sujudu hua haziwezi kufanywa isipokua na Mtu mwenye kusali. Na *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akijua juu ya tukio hili, lakini hakumkosoa wala hakumkataza wala kumrekebisha Sahaba wake huy**o.'*(Al Majmuu)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Na huu pia ndio Mtizamo wa Masahaba kina Abd Allah Ibn Umar, Abd Allah Ibn Abbas, Ibn Abu Awfah, Jabir Ibn Abd Allah, Abu Hurayrah, Aisha, *Radhi Allahu Anhum.'***

Na pia Maimamu kina Said Ibn Musayyib,Salim Ibn Abd Allah Ibn Umar, Al Qasim Ibn Muhammad, Tawus, Ataa, Makhul, Rabiah, Malik, Abu Thawr.'

Na kwa upande wa Imam Abu Muhammad Hasan Ibn Masud Al Baghawi Al Shafii basi amesema pia kua: '**Huu ndio Mtizamo wa Wengi Miongoni mwa Masahaba na Tabiina.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Al Shawqani Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Tunajua kua Kanuni ya Msingi kuhusiana na asili ya Kimumbile ya kitu hu ni Tohara, hivyo atakaesema kua kitu fulani si Tohara basi hutakiwa kutoa uthibitisho.**

Hivyo kama Mtu akija na vithibitisho vinavyokubalika kisharia basi ni vizuri, na ikiwa vyenginevyo basi hua haikibaliki Vile vile anaedai kua Damu hua Inabatilisha tohara basi hua inambidi atoe uthibitisho kama anao basi sawa kama hana madai yake hua ni batili.

Kwa tukio hua ni kikwazo kwa Sala, na Kama ikiwa Tukio litaondolewa kwa Udhu, basi hua ni lenye kuondoka hadi litakaporudia tena. **Na hakuna aliesema kua Damu inabatilisha Udhu kwa kutoa uthibitisho unaokubalika, hivyo hii inamaanisha kua kutokwa na Damu hakubatilishi Udhu.**

Kwani Al Bukhari amenukuu kutoka Kwa Jabir *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika vita vya Dhat Al Riqa, ambapo ndani yake Kuna Mtu alichomaa na Mshale wa upinde na akawa anatokwa na Damu, hivyo Mtu huyo akarukuu na kusujudu na kuendelea na Sala yake.'

Hadith hii imenukuliwa na Imm Ahmad, Imam Abu Daud, Imam Ad Daraqutni, Imam Ibn Khuzaymah, Imam Ibn Hibban na Al Hakim ameipitia na kusema kua ni Hadith sahih.'*(Al Sayl Al Jarar)*

Hivyo ingawa wengi miongoni mwa Masahaba *Radhi Allahu Anhu* na Maimamu wa Tabiina na waliofuatia baada yao akiwemo Imam Malik Ibn Anas na Wanazuoni wa Madhhab yake, Imam Muhammad Idris Al Shafii na Wanazuoni wa Madhhab yake, Imam Ahmad Ibn Hanbal na Wanazuoni wa Madhhab yake, Imam Ahu Thawr Imam Is-haq Ibn Rahawayh wanakubaliana kua Damu Inapokutoka kwenye sehemu ambayo si ya haja ndago wala kubwa hua haibatilishi Udhu.

Lakini kwa upande wa Imam Nuuman Ibn Thabit Abu Hanifa na Wanazuoni wa Madhhab yake basi wao wanasema kua: '**Kuna Hadith isemayo kua Udhu kua ni Wajib kwa kila Damu inayotiririk**a.' *(Imam Ad Daraqutni)*

Na ingawa Wanazuoni wengine wanasema kua hii ni Hadith Mursal na kuna wanaosema kua ni Dhaif lakini kwa upande wa Imam Al Tahanawi Al Hanafi basi amesema kua hii ni Hadith Sahih.

Na tunapomuangalia Imam Abu Ikhlasi Hasan Ibn Ammar Al Shurunbulali Al Hanafi basi tunaona anasema kua: '**Damu hua inabatilisha Udhu, huu ndio Mtizamo wetu na ndio pia Mtizamo wa Masahaba 10 waliobashiriwa Pepo akiwemo pia Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* pia na Masahaba wengineo.'***(Maraqi Al Falah)*

Na pia anasema Al Muhaqqiq Imam Ibn Aabidin Al Shami Al Hanafi kua: '**Kitu chochote kichafu chenye kutiririka kama Damu au Usaha kutoka kwenye Kidonda au kutoka katika sehemu yeyote ya waziYa Mwili, au kwenye sehemu ambayo itahitajika kusafishika, na kiasi ya kua ikawa inatoka kwa kiasi cha kutiririka na hivyo kutakiwa kupanguswa au kuzuiwa kwa Kitambaa basi hua ni yenye kubatilisha Udhu.'**(*Hadiyyah Al Aaliya)*

Na anasema Imam Al Kasani Al Hanafi kua: **'Ama kuhusiana na Masahaba *Radhi Allahu Anhum* waliokua wakisali huku wakiyokwa damu kwenye majeraha yao basi haya hua ni Matukio,**

yasiyojitosheleza kwani ni ya mara moja moja. Kwa mfano wakati Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alipojeruhiwa Msikitini basi haikuwekwa wazi kama alitia Udhu upya ama la,kabla ya kuendelea na Sala yake.'*(Badai Al Sanai fi Tartib Al Sharai)***

Na akasema Imam Saharanfuri Al Hanafi kua: '**Ama kuhusiana na Sahaba aliejeruhiwa wakati alipokua akisali, basi inawezekana ikawa aliotekeleza ulikua ni Mtizamo wake, au alikua hajui kuhusiana na Hukmu hii na hivyo akaendelea Kusali kutokana na kua ni mwenye kuzama ndani Utamu wa Ladha ya Mahusiano yake na Mola wake, hivyo Hadith hii haikubaliki kama Uthibitisho.'***(Badhl Al Majhud Fi Hal Abu Daud)*

Na pia akasema Al Imam BadrAl Din Al Ayni Al Hanafi kua: **'Ama kuhusiana na Hadith ya Sahaba aliepigwa Mshale na kuendelea kusali basi tunaona kua ni Ushahidi wenye Utata na hii ni kwa sababu Damu ikitiririkabasi itamuathiri Mtu husika pamoja na Nguo zake pia, na yeyote yule alieathiriwa na Damu basi Udhu wake hubatilika kutokana na Mtizamo wao***.'(Khashiyat al Ayni aAla Umdat Al Qarri)*

Ama kwa upande mwengine basi amesema Imam Attiya Sakr katika Ahsan Al Kalam Fi Fatwa wa Al Ahkam kua: **'Ingawa kuna Hadith isemayo kua: 'Kama ikiwa mmoja miongoni mwenu atatokwa na Damu Puani basi na Atoke kwenye Sala, akajisafishe na kisha atie Udhu Upya na kisha akasali tena upya" ambapo Hadith hii ni Dhaifu.**

Kuna Hadith ya Aisha Radhi Allaju Anha kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaetapika, atakaetokwa na Damu Puani, Atakaecheua au atakaetokwa na Madhii basi na akatishe Sala kisha atie Udhu na aendelee na Sala bila kuzungumza na Mtu.'*(Sunnan Ibn Majah, Sunnan Ad Daraqutni)*.

Basi Hadith hii ni Dhaifu pia, kama ilivyoelezewa na Maimamu Kadhaa. Na ni Hadith Mursal kwani Kuna Maimamu walioinukuu bila kutaja Jina la Sahaba, akiwemo Imam Ad Daraqutni,Imam Abu Hatim, na Imam Al Bayhaqi amesema kua ni Mursal Hadith

Ambapo Amesema Imam Ibn Athir kua: **'Damu ya Pua Hutoka Puani, Kutapika hua ni Kuanzia Tumboni hadi Kooni, Kucheua hua Kutoka Kooni na Mdomoni na Madhii hua ni Maji Laini meupe yatokayo katika Uume kwa Wanaume na Uke kwa Wanawake anapokua Hamu ya Matamanio lakini hua bila ya Kutiririka.'**

Abbad Ibn Bishr alijeruhiwa na Upinde akiwa ndani ya Sala na hivyo akamalizia SalaAnas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* anasema kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifanya Hijama na Hakutia Udhu baada yake, na Wala hakukosha sehemu alizofanyiwa Hijama. Hii pia ni Hadith Dhaifu.'*****(***Ahsan Al Kalam Fi Fatwa wa Al Ahkam)*

Hivyo Vithibitisho hivi vya Hoja zote vinatuonesha kwanini Wanazuoni wakatofautiana Mtizamo juu ya Jambo hili ambalo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Al Shafii na Imam Hanbal wanasema kua: Damu itokayo kwenye Jeraha lisikokua kwenye Sehemu za Siri haibatilishi Udhu wala Sala. Na Wanazuoni wa Madhhab Imam Abu Hanifa wanasema kua: Inabatilisha

Kwani Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu kua:

﴿قُل لاَّ أَجِدُ فِي مَآ أُوْحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّماً عَلَىٰ طَاعِمٍ يَطْعَمُهُ إِلاَّ أَن يَكُونَ مَيْتَةً أَوْ دَماً مَّسْفُوحاً أَوْ لَحْمَ خِنزِيرٍ فَإِنَّهُ رِجْسٌ أَوْ فِسْقاً أُهِلَّ لِغَيْرِ ٱللَّهِ بِهِ فَمَنِ ٱضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلاَ عَادٍ فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

Qul la ajidu feema oohiya ilayya muharraman AAalataAAimin yatAAamuhu illa an yakoona maytatan aw daman masfoohan aw lahma khinzeerin fa-innahu rijsun aw fisqan ohilla lighayri Allahi bihi famani idturra ghayra baghin wala AAadin fa-inna rabbaka ghafoorun raheemun*(Surat Al Anaam 6:145)*

Tafsir: ***Sema (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) KuaSikuona Katika Kile nilichoshushiwa Kilichokatazwa Kuliwa Kwa Watu wanaotakakukilaIsipokua kama Ikiwa ni MaitiAu Damu Yenye Kutiririka Au Nyama ya Nguruwe Kwani Kwa hakika Hivyo Sio Tohara Au Nyama isokua Halali iliyochinjwaBila Kutajiwa Jina la Allah Subhanah wa Ta'ala Lakini Yeyoye yule atakaekua na Dharura Na Akawa Hana Njia Nyenyinge isipokua kuasi (Kwa kula hivyo vilivyotajwa)Wala si kutokana na Matamanio basi kwa Hakika Mola wako Ni mwingi wa Msamehevu na Mwingi wa Huruma.***

Na kama tunavyoona kua ayah ii metaja aina ya Damu ambayo ni *Daman Masfoohan* ambapo neno Masfuuhan ni neno lenye kutokana na neno *Safaha* lenye kumaanisha Kumiminika, Kutiririka au Iliyokatikahali ya kua ni ye kumwagwa au kumwagika.

Ambapo anasema Imam Tawus kuhusiana na kushushwa kwa Aya hii kua amesema Baba yake kua: **'Mapagani wa kiarabu walikua ni wenye kutangazia uharamu wa vitu kutokana na matamanio yao kwa mfano kuna baadhi ya Wanyama hua ni halali kwa Wanaume lakini ni Haram kwa Wanawake wao. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha Ayah hii.'**

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Din Mujtahid Imam, Imam Muuhammad Idris Al Shafii anasema kua;**'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa kuhusiana na Uhalali wa baadhi ya vitu, katika wakati alipokua katikamji wa Makkah, hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamshushia Aya hii kumaanisha kua hakuona chochote katika aliyoshushiwa kuhusiana na vilivyoharamishwa isipokua hivyo vilivyotajwa kwenye Aya hii, na ndio maana aya hii ikawa ni yenye kuchagua maneno haya maalum kua 'Sikukuta mimi chochote kile katika aya nilizoshushiwa kilichoharamishwa.'**

Na aya imesema hivyo kwa sababu makatazo mengine juu ya vyakula vilivyoharamishwa yalifuatia katika kipindi cha baada ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua ni mwenye kuishi katika Mji wa Madina.

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema tena Katika Qur'an kua:

إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ ٱلْمَيْتَةَ وَٱلدَّمَ وَلَحْمَ ٱلْخِنزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ بِهِ لِغَيْرِ ٱللَّهِ فَمَنِ ٱضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلاَ عَادٍ فَلآ إِثْمَ عَلَيْهِ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

Innamaharrama AAalaykumu almaytata waalddama walahma alkhinzeeri wama ohilla bihi lighayri Allahi famani idturra ghayra baghin wala AAadin fala ithma AAalayhi inna Allaha ghafoorun raheemun*(Surat Al Baqara 2:173)*

Tafsir: ***Amekukatazeni Nyinyi Maiti, na Damu na Nyama ya Nguruwe na kile ambacho hakikuchinjwa*** **Kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Lakini Yeyoye yule atakaekua na Dharura Na Akawa Hana Njia Nyengine isipokua kuasi (Kwa kula hivyo vilivyotajwa) Wala si kutokana na Matamanio basi kwa Hakika Mola wako Ni mwingi wa Msamehevu na Mwingi wa Huruma.**

Na kisha aya inayofuatia ikajumuisha kuhusiana na vilivyoharamishwa pale iliposema:

﴿حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ ٱلْمَيْتَةُ وَٱلْدَّمُ وَلَحْمُ ٱلْخِنْزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ لِغَيْرِ ٱللَّهِ بِهِ وَٱلْمُنْخَنِقَةُ وَٱلْمَوْقُوذَةُ وَٱلْمُتَرَدِّيَةُ وَٱلنَّطِيحَةُ وَمَآ أَكَلَ ٱلسَّبُعُ إِلاَّ مَا ذَكَّيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى ٱلنُّصُبِ وَأَنْ تَسْتَقْسِمُواْ بِٱلأَزْلاَمِ ذٰلِكُمْ فِسْقٌ ٱلْيَوْمَ يَئِسَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ مِن دِينِكُمْ فَلاَ تَخْشَوْهُمْ وَٱخْشَوْنِ ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلإِسْلاَمَ دِيناً فَمَنِ ٱضْطُرَّ فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرَ مُتَجَانِفٍ لِإِثْمٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

Hurrimat AAalaykumu almaytatu waalddamu walahmu alkhinzeeri wama ohilla lighayri Allahi bihi waalmunkhaniqatu waalmawqoodhatu waalmutaraddiyatu waalnnateehatu wama akala alssabuAAu illa ma dhakkaytum wamadhubiha AAala alnnusubi waan tastaqsimoo bial-azlami dhalikum fisqun alyawma ya-isa alladheena kafaroo min deenikum fala takhshawhum waikhshawni alyawma akmaltu lakum deenakum waatmamtu AAalaykum niAAmatee waradheetu lakumu al-islama deenan famani idhtturra fee makhmasatin ghayra mutajanifin li-ithmin fa-inna Allaha ghafoorun raheemun*(Surat Al Maidah 5:3)***

Tafsir: **Mmeharamishiwa juu yenu Maiti na Damu na nyama ya Nguruwe na kile ambacho kimechinjwa si kwa ajili ya Allah, na kilichonyongwa au kupigwa kwa kipigo cha nguvu, au kwa kuangukia Kichwa, au kwa Kutobolewa na Pembe za Mnyama mwengine, na kile kilichobakia baada ya kuliwa na Wanyama wengine isipokua kama mtawahi kukichinja (kabla hakijafa). Na kile ambacho kimechinjwa kwa kutolewa kafara kwenye Madhabahu ya Masanam. Na pia kutumia mishare kwa ajili ya kutafuta bahati au kutoa maamuzi, yote hayo ni Uasi. Leo hii Wasioamini wote wameishiwa na matumaini juu ya Dini yenu, hivyo msiwe na khofu nao, bali kuweni na khofu nami. Leo hii nimeikamilisha Dini yenu, nimekamilisha fadhila zangu juu yenu na nimeuchagua Uislam kua ndio Dini yenu. Lakini kwa yule ambae atakumbana na Njaa kali (basi anaweza kula hivyo vilivyokatazwa), bila ya (kua ni mwenye) kuelemea kwenye dhambi, na kwa hakika Allah ni mwingi wa Kusamehe na ni mwingi wa Rehma.**

Ambapo iliposhuka aya hii basi Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* basi alilia sana kutokana na kujua kua umewadia mda wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuondoka Duniani kwani ameshatimiza wajibu wake wa kufikisha ujumbe wake kutoka kwa Mola wake kwa ajili ya viumbe wake. Na bila ya shaka hili lilikua sahih kwa sababu mara baada ya kushuka aya hii basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliishi kwa mda wa siku 81 tu.

Ambapo Wanazuoni wanakubaliana kua Wanyama waliohalalishwa pia wamo Sungura, Mjusi wa Jangwani, na Nzige.

Ama kuhusiana na walioharamishwa basi ni wale wenye kuchana Vyakula vyao au Wanyama wao, na hii ni kutokana na Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ يُوسُفَ، أَخْبَرَنَا مَالِكٌ، عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، عَنْ أَبِي إِدْرِيسَ الْخَوْلاَنِيِّ، عَنْ أَبِي ثَعْلَبَةَ ـ رضى الله عنه ـ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم نَهَى عَنْ أَكْلِ كُلِّ ذِي نَابٍ مِنَ السِّبَاعِ

‘Amesema Abd Allahi IbnYusuf kua ametuambia Malik Kila kua amesema Ibn Abi Shihab kua amesema Abi Idrisa Al Khawlani kua amesema Abu Thalabah *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua : Mnyama wa Mwituni anaetumia Kucha zake ni Haram kumla’’*(Bukhari na Muslim)*

Ndege Mwitu yaani wale wenye kuwachanachan Wanyama wenzao kwa Kucha zao na kuwala, kama alivyosema hadith ifuatayo:

عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ كُلِّ ذِي نَابٍ مِنَ السِّبَاعِ وَكُلِّ ذِي مِخْلَبٍ مِنَ الطَّيْرِ. رَوَاهُ مُسْلِمٌ

Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameharamisha kila Mnyama wa Mwitu anaetumia Kucha na kila Ndege mwenye kutumia Kucha.’*(Sahih Muslim)*

Nyama ya Punda ni haramu kulingana na Mtizamo wa Madhhab yote ambapo kwa upande wa Nyama ya Farasi basi hua ni yenye kukirihisha kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik. Mbwa, Kima, Tembo na Paka ni Haram kulingana na Madhhab yote manne. Mbwa mwitu ni haram kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanfa, Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Na kila kinachotambaa kama Panya, Nyoka, Nge, Tandu, Chura, Popo, Kinyonga, Mende, Minyoo, Funza, Nyungu Nyungu, Bui bui n.k.

Jallalah yaani Mnyama anaekula kinyesi cha Wanyama wengine ni haramu kula Nyama yake, Maziwa yake na hata Mayai yake, labda iwe Mnyama huyo amedhibitiwa na kufugwa na kupewa chakula cha kawaida kwa mda kama wa miezi 6.

Na ni haramu pia kwa Wanyama wote wanaokula Nyama, na kila kilicho kichafu kwani *Allah Subhanah wa Ta’ala* amesema katika Qur’an kuhusiana na kila kisicho kisafi kua:

ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلأُمِّيَّ ٱلَّذِى يَجِدُونَهُ مَكْتُوباً عِندَهُمْ فِى ٱلتَّوْرَاةِ وَٱلإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُم بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ ٱلْمُنْكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ ٱلْخَبَآئِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَٱلأَغْلاَلَ ٱلَّتِى كَانَتْ عَلَيْهِمْ فَٱلَّذِينَ آمَنُواْ بِهِ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِىۤ أُنزِلَ مَعَهُ أُوْلَئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ

Alla<u>dh</u>eena yattabiAAoona alrrasoola alnnabiyya al-ommiyya alla<u>th</u>ee yajidoonahu maktooban AAindahum fee alttawr<u>a</u>ti waal-injeeli ya/muruhum bialmaAAroofi wayanh<u>a</u>hum AAani almunkari wayu<u>h</u>illu lahumu al<u>t</u>tayyib<u>a</u>ti wayu<u>h</u>arrimu AAalayhimu alkhaba-idha waya<u>d</u>aAAu AAanhum i<u>s</u>rahum waal-aghl<u>a</u>la allatee k<u>a</u>nat AAalayhim faalla<u>dh</u>eena <u>a</u>manoo bihi

waAAazzaroohu wanasaroohu waittabaAAoo alnnoora alladhee Unzila maAAahu ola-ika humu almuflihoona.*(Surat Al Araf 7: 157):*

Tafsir: **Wale wanaomfuata Mtume Nabii ambae hajui kusoma wala kuandika ambae wamemuona ameandikwa kwenye Taurat (katika Deut, xviii, 15) na Injil (katika Gospel) (John xiv, 16) anaewaamrisha Mema na Kuachana na Maovu, amewahalalishia *Tayyibat* (Vilivyo vizuri) na kuwakataza *Khabaith* (Vilivyo vichafu) amewaokoa kutokana na Mzigo mzito sana na kutokana na minyororo waliyofungwa. Hivyo wale waliomuamini *(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam)*na kumuheshimu na kumsaidia na kufuata Nuru aliyoshushiwa, basi ndio wao watakaofuzu**

Hivyo kulingana na Aya hizi basi Damu hua ni Uchafu, na ingawa hali iko hivyo Lakini hata Hivyo Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Uchafu wa Damu na sehemu Inayotokea au sehemu iliyopo.

Ambapo kwanza Damu itokayo katika sehemu mbili za Siri hubatilisha Udhu iwe ndani ya Sala au Nje ya Sala. Iwe Nyingi au Kidogo iwe ni iliyosababishwa na Minyoo, au Maumbile au Kijiwe n.k.

Hivyo Na anasema Imam Ahmad Zayn Ad Din Al Malibari Al Shafii katika kitabu chake cha Fat-h Al Muin kua: **'Na Yanayobatilisha Udhu ni Manne, ambayo ni Kua na Hakika kua Kuna kitu zaidi ya Madhii kua kimetokaIwe cha Kuchuruzika au cha Gesi, Iwe cha Maji Maji au Kikavu, iwe kama kawaida kama Mkojo, Au Hata Damu kutokana na Bawasili n.k.'***(Fat-h Al Muin)*

Na hivyo hivyo ndio alivyosema Imam Abd Allah Ibn Abd Rahman Ba Fadhl Al Hadhrami Al Shafii katika Sharh Al Muqaddimat Al Hadhramiya maarufu kama *Bushra Al Karim Bi Sharh Masail Tarim.* Hivyo juu ya hili kuna Makubaliano ya Wanazuoni wote. Tofauti ipo katika Aina ya Pili ya Damu Itokayo katika sehemu Nyenginezo Mwili, kama kwenye Jeraha, Kidonda n.k na kua Nje ya Sala na Ndani ya Sala.

Ambapo kuhusiana na Mtu anapokua Nje ya Sala basi amesema Shaykh Ul Islami Imam An Nawawi kuhusiana na hili kua: '**Hakuna Tatizo la Kubatilika kwa Udhu wa Mtu kutokana na kutokwa Na Damu katika sehemu zisizokua za Siri**.'*(Al Majmuu)*

Ambapo kuhusiana na Ndani ya Sala basi Wanazuoni wanasema kua: '**Sala Habatiliki Kutokana na Kutokwa na Damu kwenye Kidonda, Jeraha n.k pale Inapokua kuna hali zifuatazo:**

1-Damu hio ni ya Mtu husika anaetokwa nayo.

2-Damu Hio haitoki kwa Kukusudiwa.

3-Damu hio haisambai katika Sehemu nyengine zaidi ya Inapotokea.

Hivyo Damu inapokua katika hali hizi na si *daman masfoohan*basi hua Haiifisidi sala ya Mtu husika wala udhu wa mtu husika.

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam An Nawawi baada ya Kunukuu Hadith ya Abbad Ibn Bishr *Radhi Allahu Anhu* basi anasema kua: **'Hadith inathibitisha kua Sahaba huyu hakutokwa na Damu Nyingi kiasi ya kuzirovya Nguo zake, kwani ni Damu kidogo tu ndio iliyogusa nguo zake jambo ambalo hua linakubalika kutokana na Dharura, na hivi ndivyo walivyosema As-hab Al Wujuh wetu.'***(Al Majmuu)*

Ambapo kuhusiana na Damu ya Pua basi ikiwa kidogo hua haina madhara lakini kama ikiwa nyingi basi inabidi Mtu akatishe Sala yake kama anavyosemaImam Al Muhaqqiqin Al Faqih Al Allamah Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: '**Kama Mtu atakua anatokwa na Damu Puani kama ni Kidogo basi hua haina Dhara.'**

Lakini kama ikiwa Damu ni Nyingi basi Mhusika hua na Wajibu kukatisha Sala, hata kama Sala hio itakua ni Sala ya Ijumaa, hii hua ni tofauti na wale wanaokua na shaka nayo, au kabla yake au baada yake na kama Mtu atakua na Matumaini kua itakata na mda bado upo basi na aisubiri ikate.'*(Tuhfah Al Muhtaj)*

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii na As-hab Al Wujuh (Wanazuoni wa Msingi wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii). Kwa maana hio basi kama itakua Mtu anasali na kisha akatokwa na Damu ya Pua na kisha akaifuta au akaizuia kwa Kitambaa Au Tishu na Ikasita Kutoka basi hua anaendelea na Sala bila tatizo.

Ila kama ikiwa nyingi haikati basi mhusika itambidi akatishe Sala akajisafishe na kisha atarudi na kuendelea na Sala.

Na anasema Al Imam Al Khatib Al Shirbini kua: '**Na miongoni mwa Vilivyoruhusika kwa ugumu wa kujiepusha navyo kwa mfano Mtu anapita kwenye Njia ambayo Ina Matope ambayo yana Uchafu, kutokana na Kutokua na Njia nyegine ya Kuyaepuka.**

Na kinachokubalika kwa dharura hua ni kulingana na Sehemu na Wakati, kama Nguo na Mwili, Kama Kijipu na wadudu kama Chawa na Damu, pia Hijama na Sehemu husika za Mwili na pia Kinyesi cha Nzi hata kama kikiwa ni kingi.

Hata Kama Damu kutokana na Kutawanyika kwa Mshipa wa Damu yaani Wingi wake kulingana na ujumla wa kiathari na wala si kulingana na Kitendo kilichofanyika labda kwa Kumuu Nzi au Kukibinya Kidonda basi hii hua haitokubalika kwa sababu ya wingi wa Damu kulingana na Mazoea ya Watu,kama alivyosema Imam Al Rafii na Imam An Nawawi katika Al Majmuu.

Na kuhusiana Damu ambayo sio yake Mtu na isiokua Kidogo yaani Kama Damu ya Mbwa kutokana na Uzito wake.

Na Kama Damu Usaha, Maji ya Kidonda, au Kitu chenye Harufu mbaya, na hivyo kama Mtu akasali na kitu kisichokubalika na yeye hajui au anajua lakini amesahau na kisha akakumbuka basi kaa Mtu huyo hua ni lazima kwake Kuirudia Sala yake, na kila Sala ambayo aliisali hukua akiwa na hakika kua alikua ni Uchafu.' *(Al Iqna Fi Hal Al Faaz Abi Shujaa)*

Naam anasema Imam Malik Ibn Anas muanzilishi wa Madhhab ya Imam Malik kua: '**Ameniambia mimi Yahya kua amesema Malik kua amesema Nafi'i kua:**

أَنَّ عَبْدَ اللهِ بْنَ عُمَرَ كَانَ إِذَا رَعَفَ انْصَرَفَ فَتَوَضَّأَ ثُمَّ رَجَعَ فَبَنَى وَلَمْ يَتَكَلَّمْ

Wakati Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alipokua na tatizo la kutokwa Damu Puani basi huondoka na Kutia Udhu na kisha hurudi na kuendelea na Sala bila ya Kuzungumza na Mtu.' *(Muwatta Imam Malik)*

Amesema tena Imam Malik Ibn Anas kua:

«أَنَّهُ بَلَغَهُ أَنَّ عَبْدَ الله بْنَ عَبَّاسٍ كَانَ يَرْعُفُ فَيَخْرُجُ فَيَغْسِلُ الدَّمَ عَنْهُ ثُمَّ يَرْجِعُ فَيَبْنِي عَلَى مَا قَدْ صَلَّى

‘**Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ilikua kila alipokua na tatizo la kutokwa Damu Puani basi hutoka nje na Kukosha Pua yake na kisha Hurudi na Kuendelea na Sala yake’***(Muwatta Imam Malik)*

مَالِك عَنْ يَزِيدَ بْنِ عَبْدِ الله بْنِ قُسَيْطٍ اللَّيْثِيِّ «أَنَّهُ رَأَى سَعِيدَ بْنَ الْمُسَيّبِ رَعَفَ وَهُوَ يُصَلِّي، فَأَتَى حُجْرَةَ أُمِّ سَلَمَةَ زَوْجِ النَّبِيِّ صَلَّى الله عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، فَأُتِيَ بِوَضُوءٍ فَتَوَضَّأَ، ثُمَّ رَجَعَ فَبَنَى عَلَى مَا قَدْ صَلَّى»

Amesema Yazid Ibn Abd Allah Ibn Qusayt Al Layth kua: ‘Nilimuona mimi Said Ibn Musayyib akiwa na Matatizo ya Kutokwa na Damu Puani wakati alipokua Akisali. **Hivyo alienda kwenye Chumba cha Ummu Salamah, Mke wake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,*na akaletewa Maji ya Kutia Udhu na akatia Udhu, na kisha akarudi katika sehemu aliyokua Akisalia na Kuendelea na Sala yake.’***(Muwatta Imam Malik)*

Na pia kuna Hadith isemayo:

عَنْ هِشَامِ بْنِ عُرْوَةَ، عَنْ أَبِيهِ، «أَنَّ الْمِسْوَرَ بْنَ مَخْرَمَةَ أَخْبَرَهُ: أَنَّهُ دَخَلَ عَلَى عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ مِنْ اللَّيْلَةِ الَّتِي طُعِنَ فِيهَا فَأَيْقَظَ عُمَرَ لِصَلَاةِ الصُّبْحِ، فَقَالَ عُمَرُ: نَعَمْ، وَلَا حَظَّ فِي الْإِسْلَامِ لِمَنْ تَرَكَ الصَّلَاةَ. فَصَلَّى عُمَرُ وَجُرْحُهُ يَثْعَبُ دَمًا

Anasema Hisham Ibn Urwa kua amesema Baba yake kua amesema Miswar Ibn Makhramah kua:Niliingia Mimi kwa Umar Ibn Al Khattab katika Usiku aliochomwa Upanga, hivyo nikamuamsha Umar kwa ajili ya Salat Al FajrNa Umar akasema: Naam Hakuna sehemu ya Uislam kwa Mwenye kuacha Sala. **Hivyo Umar Ibn Al Khattab akasali huku Jeraha lake likiwa ni lenye kutoka Damu.’***(Muwatta Imam Malik)*

Hivyo kwa Mtu mwenye Tatizo la Kutokwa na Damu Puani basi anatakiwa aipanguse Damu hio, na kama Damu hio Haikati basi Mtu husika anaruhusika kutoka na kuenda kuikosha Pua yake na kisha na arudi na kuendelea na Sala yake.

Ambapo anasema Imam Muhammad Al Zarqani Al Maliki kuhusiana na Hadith hizi kua: **‘Hivyo Vitendo vya Masahaba havioneshi kua Damu ya Pua hua Inabatilisha Sala, na hivyo kama Mtu huyo akitoka na kuenda Kukosha Pua yake bila ya Kuzungumza na Mtu katika Masafa ambayo si ya Mbali basi anaweza kurudi na kuendelea na Sala yake.**

Na kama anachokitambaa basi anaweza Kuifuta Damu hio na kisha akaendelea na Sala yake.Ambapo Imam Malik Ibn Anas Anaendelea kusema kua: Amesema Salim Ibn Abd Allah kua amesema Malik kua amesema Abd Rahman Ibn Mujbir kua: Alimuona Salim Ibn Abd Allah akiwa Anatokwa na Damu Puani mpaka Vidole vyake vikawa vinadamu hio kutokana na kuipangusa na huku akisali bila ya Kuenda Kutoa Udhu Upya.’*(Muwatta Imam Malik)*

Na akasema Imam Ibn Zayd Al Qayrawani Al Maliki kua: **'Yeyote yule atakaekua na Tatizo la Damu ya Puani wakati akiwa nyuma ya Imam, basi na atoke na kisha akakoshe Damu hio.**

Na wakati akiwa hajazungumza wala hajakanyaga Najis, Na Hatakiwi Kuiendeleza Rakaa ambayo hakuimalizia kwa Sijda mbili, kwani Anatakiwa asiihesabu, Na hatakiwi Mtu kukatisha Sala kutokana na Damu kidogo bali anatakiwa aiwache ikauke isipokua pale itakapokua inachuruzika.'*(Risala Al Qayrawanniyah)*

Ambapo amesema Ima Al Baji Al Maliki kua:**'Kuna Makubaliano ya Masahaba Wanazuoni kua Kutokwa na Damu Puani hakubatilishi Sala.'**

Hivyo ingawa Kutokwa na Damu Puani hua Hakubatilishi Sala lakini hua inatakiwa Damu hio Ifutwe.

Kama anavyosema Imam Al Shirbini kua: **'Na kua na Usafi kutokana Na Uchafu ambao hauwezi Kudharaulika kwenye Mavazi yake Mtu, Mwili wake, au hata Ndani ya Pua yake au Mdomo au Machoni au Masikioni au katika sehemu anayosalia.**

Kwani Sala yake hua batili ikiwa Kuna uchafu katika sehemu hizo hata kama ikiwa Mtu hajui kuwepo kwa Uchafu huo au kubatilika huko na hii ni kwa Sababu ya kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema na Mavazi yenu yatoharisheni.

Na ndani ya Pua na Ndani ya Mdomo hua kunahesabika kama Nje yake.'*(Al Iqna Fi Hal Al Faaz Abi Shujaa)*

Hivyo kama Damu itakua Inatoka basi inatakiwa kufutwa na kama ni kidogo basi itakauka na haina tatizo.Ila kama damu itakua bado inaendelea Kutoka haikati na Mda wa Sala Unapita basi unaweza Kusali katika hali uliyokua nayo. Ambapo hapa Wanazuoni wamechukulia mfano wa kiasi ya Hadith ya Sayyidna Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu.*

Na Wanazuoni wamekisia udogo wa Damu isiyobatilisha Udhu na Sala kua ni kulingana na Ukubwa wa Dirham moja ya Ghuli au Sehemu ya Ndani ya Kwato ya Punda au mzunguko wa mueneo wake usizidi Sentimita 4.

Na Baadhi yao wakasema kua Udogo wake hua ni kulingana na Dasturi za Jamii ya Watu kuhusiana na Udogo wa Kutokwa na Damu.

Na ndio Maana wakasema Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua: Kama Ikiwa Mtu atahisi kua anatoka Damu Puani na kisha akatia ndani Puani kidole chake na kikitoa huku kikiaa kina Rangi ya Damu, basi Udhu wa Mtu huyo hua haujatenguka hadi pale itakapokua Damu hio inachuruzika.

Au kama Mtu akipenga Pua na kisha ikaruka Damu kidogo kutoka ndani yake basi Udhu wa Mhusika hua haujakatika.'*(Radd Al Mukhtar)*

Na anasema Imam Sulayman Al Bajuri Al Shafii kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu kutokana na Damu kua: '**Kama ikiwa tone la Damu au la Usaha si ya Mtu husika bali ni ya Mtu mwengine au ya Mnyama asiekua Mbwa wala Nguruwe, au ya Mdudu kama mbu basi hua haibatilishi Udhu wala Sala ya Mhusika.**

Lakini kama Damu ikiwa ni ya Mtu husika basi hata akama ikiwa Nyingi hua haiathiri Udhu wa Mhusika wala Sala pale itakapokua kuna hali zifuatazo kimasharti:

1-Damu hio haikusababishwa kutoka kwa Makusudi, kama vile Mtu kujikamua au Kujichinja.

2-Damu hio iwe haikuchanganyika na kitu chengine chochote, yaani hata kama kitu hicho kiwe ni tohara.

3-Damu hio iwe haijachuruzika kutoka kwenye Jeraha kufikia kiasi ya masafa ya juu ya Ngozi au juu ya Nguo ya Mhusika.

Kwa Mfano labda tuseme Damu itokayo kwenye Jeraha la kichwani kuangukia kwenye Mikono au Miguu (ambapo hali hua ni tofauti kama Damu hio ikiangukia na maeneo ya karibu na kichwa kama Usoni, Shingoni au Begani).

Hivyo Kama ikiwa Masharti haya hayakutekelezeka kuhusiana na Damu hio ya mhusika basi ni Damu kidogo tu ndio itakayokua inaruhuika kutokana na kua haitobatilisha Udhu wa Mtu husika, lakini kama ikipitiliza Masharti hayo basi Udhu utabatilika.

Ama kuhusiana na kiasi cha udogo wa Damu kidogo basi hua ni Kulingana na Dasturi za watu husika.

Yaani kama itakavyokua kiasi fulani kinahesabika kua ni kidogo kaa utokaji wa damu ambacho hua tofauti na kiasi cha wingi wa utokaji wa Damu kulingana nao watu katika Jamii husika.'*(Hashiyah Al Baijuri).* Na Mtizamo huu pia ndio ulioelezewa na Imam Abd Allah Ibn Abd Rahman Ba Fadhl katika *Bushra Al Karim bi Sharh Masail Tarim.*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Quduri Al Hanafi basi nae anasema kua: **'Miongoni mwa yanayobatilisha Udhu hua ni Damu au Usaha pale utakapotoka na kufikia hadi katika sehemu ya kiungo cha mwili ambacho kinatakiwa Kitiwe Maji katika Kutia Udhu.**'*(Al Lubbab Fi Sharh Al Kitab)*

Yaani kwa mfano kama ikiwa Mtu atajichuna kwa bahati mbaya kwenye Bega na akatoka Damu ambayo ikachuruzika hadi kwenye Kisugudi cha Mkono wake, basi hapo Udhu utabatilika.

Kwa maana hio basi kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kama ikiwa Mtu atatokwa na Damu ya Pua na kisha Damu hio ikawa haikufutwa na kufikia hadi kwenye sehemu ya ndani ya Pua ambayo hua inatakiwa kutiwa Maji katika wakati wa Kutia Udhu.

Hivyo kama Mtu huyo alikua na Udhu basi baada ya kufikwa na hali hio itambidi atie udhu yena upya. Kwani imesemwa katika *Raad Al Mukhtar* kua: **'Wakati Damu itakapochuruzika kwenye Pua basi hata kama ikiwa ni sehemu ya Juu tu ya Pua basi Udhu hubatilika'.**

Ama kuhusiana na Damu ya Maiti wa Kiislami alieuliwa kwenye Vita vya Jihad kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua ni Tohara pale inapokua imegandana nae na hii ni kulingana na mtizamo wa Madhhab Ya Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad Ibn Hanbal.

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- HEDHI

❖❖❖❖

Tumeangalia kuhusiana na kubatilika kwa Udhu kutokana na Damu, ambapo tumeona kua kuna Damu aina Mbili. Kwanza Damu itakayotoka kwenye Sehemu za Siri iwe kwa Mwanammke au Mwanamme hua inabatilisha Sala.

Na kuna Damu ambayo inasifa ya kua ni Daman Masfuuhan yaani yenye kutirirka na kutapakaa ambayo pia inabatilisha Udhu na Sala. Kwa maana hio basi Damu isiyokua na Sifa ya Kutotiririka na hivyo haitapakai zaidi ya Sehemu iliyotoka kwenye Jeraha lake hua haibatilishi Udhu wa Sala.

Hivyo kabla kuendelea zaid basi na tufafanue kuhusiana Damu zitokazo kwenye Sehemu za Siri kwa upande wa Wanawake ambazo hubatilisha Udhu. Kwa sababu Wanawake wenyewe wengi sana hua zinawachanganya hivyo ni muhimu kukumbushana ili tupate kua salama katika Ibada zetu ikiwemo Sala na Funga pia.

Na Kujua Juu ya Haya hua si kwa Wanawake peke yao tu, bali pia hua kwa Wanaume pia kwani nao wana Wake na hivyo wanatakiwa wajue kuhusiana na Wake zao kama Wanaruhusika Kusali ama la, kufunga ama la, Kuingiliana nao Ama la, na pia Wanuame ni wazee wa watoto wa Kike, hivyo inatakiwa wajue pia kwanini Binti yake hakusali katika siku husika n.k.

Anasema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: '**Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: Mayahudi walikua wakijitenga na Wanawake zao katika kipindi cha wakati wa siku zao za Mwezi, kiasi ya kua walikua wakikataa hata kukaa nao pamoja kwenye Meza zao katika wakati wa kula, hivyo Maansari nao wakaathirika na jambo hilo na wao pia wakaanza kufanya hivyo hivyo kwa wake zao. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaulizwa kuhusiana na jambo hilo na hivyo *Allah Subhana wa Ta'ala* akamshushia *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* aya hii ambayo inasema:**

﴿وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ ٱلْمَحِيضِ قُلْ هُوَ أَذًى فَٱعْتَزِلُواْ ٱلنِّسَآءَ فِى ٱلْمَحِيضِ وَلاَ تَقْرَبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ ٱللَّهُ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ ٱلْمُتَطَهِّرِينَ﴾

Wayas-aloonaka AAani almaheedhi qul huwa adhan faiAAtaziloo alnnisaa fee almaheedhi wala taqraboohunna hatta yat-hurna fa-idha tatahharna fa/toohunna min haythu amarakumu Allahu inna Allaha yuhibbu alttawwabeena wayuhibbu almutatahhireena *(Surat Al Baqara 2:222)*

*Tafsir: '**Na wanakuuliza kuhusiana na Hedhi waambie kua: 'Ni Adha, hivyo kaeni mbali na Wanawake wanapokua katika Hedhi na msiwakaribie mpaka wawe tohara. Na kisha watakapojitoharisha basi waingilieni katika sehemu aliyokuamrisheni Allah, kwani kwa hakika Allah anawapenda wenye kufanya toba na wenye kujitoharisha.''***

Hii ni miongoni mwa aya 2 ambazo zimetumia neno *Mahiidh* ambalo ni lenye kutokana na neno *Hadhat* ambalo hua linamaanisha Kua katika Njia yake, Kua katika Siku zake, Kua katika Hedhi, Kutoka Damu kwenye Fuko la Uzazi, hivyo neno *Mahiidh* hua linamanisha Wakati wa Kutoka Damu, Sehemu ya Kutoka Damu.

Hivyo kuhusiana na Damu basi kunaaina Tatu za Damu ziwatokazo Wanawake kimaumbile ambazo ni Hedhi, Istihadhah Na Nifas.Na kulingana na Kitabu cha *Fiqh Al Minhaji Ala Madhhab Al Imam Al Shafii* basi tunaona kua:

حيض في اللغة: السيلان. يقال حاض الوادي إذا سال. وفي الشرع: دم جبلة ـ أي خلقة وطبيعة ـ تقتضيه الطباع السليمة يخرج من أقصى رحم المرأة بعد بلوغها على سبيل الصحة، في أوقات معلومة

Neno *Haydh*Kilugha hua linamaanisha Kutiririka, ambapo kwa Kisharia hua linamaanisha kua ni Damu inayotiririka kutoka katika Uke wa Mwanammke mwenye Uzima wa Afya ambae amefikia Umri fulani wa Kubaleghe.

Ambapo *Shaykh Al Akbar Imam Muhyi Ad Din* Abu Bakar Ibn Arabi amesema kua: '**Kuna aina nane za majina ya Mwanamke mwenye Hedhi ambayo ni Haidh, Aarik, Farik, Tamis, Daris, Kabir, Dhahik na Tamith.**'

Kwa maana hio basi Hedhi hua ni Damu ambayo inamtoka Mwanamke mzima mwenye Afya yake na katika hali ya kawaida ya Kimaumbile.Hivyo Damu yeyote itakayomtoka Mwanammke katika uke wake katika hali isiyokua ya kawaida basi hua ni tatizo au maradhi na hua haiwezi kuhesabiwa kua ni Hedhi.

Na hivyo aina hii ya Damu isiyokua ya Hedhi hua inajulikana kama *Fasad* au *Istihadhah.***Ambapo Kisharia basi neno Istihadhah ni lenye kumaanisha Damu inayotoka katika Uke wa Mwanamke kutokana na Maradhi au kutokana na Tatizo la kupasuka Mshipa wa Damu katika Mlango wa Uke ambao hujulikana kama Al Adhil.**

Na Neno Nifas linatokana na Neno Nafs yaani Nafsi, na hii ni kwa Sababu kwa Lugha ya Kiarabu neno Nafsi hua pia linamaanisha Damu. Ambapo Damu hii hua ni yenye kutoka kabla tu ya kutaka Kujifungua, katika Kujifungua na baada ya kujifungua kwa Mwanammke. Hivyo hua ni yenye kuambatana na hatua za Kuzaliwa kwa Mtoto aliefikia mda wake wa kuzaliwa.

Ambapo Mwanammke aliekua katika hali kama hii ya kutaka kujifungua na kuanza kutokaa na Damu ya Nifasi hua anajulikana kama Nufasa, yaani Mwenye kutiririkwa na Damu ya Uzazi.Na Mwanamke huyu hua ni Tanfis yaani Aliepata Afueni kutokana na Uzito wa Kujifungua.

Na mbali ya kua Damu ya Nifasi hua ni yenye kuambatana na hatua za Kuzaliwa kwa Mtoto aliefikia mda wake wa kuzaliwa lakini pia Nifas huhesabiwa kama Damu ambayo itamtoka Mwanamke aliekua Mja mzito na akajifungua katika Kipindi ambacho hata kama Mtoto aliezaliwa hukuwahi kupindi cha kawaida cha kuzaliwa yaani hata katika kipindi ambacho kitakachozaliwa kitakua hakijawa na umbo la mtu bado, tuseme labda ni *Aalaqah* tu yaani Pande la Damu au ni M*udghah* yaani pande la Nyama tu.

Hivyo tunapoangalia juu ya haya basi tunaona kua Mwanamke huweza kua na Hali zifuatazo kisharia kulingana na Maumbile yao:

1-Hua na hali ya kua Tohara yaani ila ya kutokwa na Damu yeyote.

2-Hua na hali ya kua na Hedhi katika wakati maalum na hali maalum.

3-Hua na hali ya kua na Istihadhah. Yaani kupita mda wa kawaida katika kutokwa na Damu kulingana na Mzunguko wa Hedhi.

4-Hali ya Kua na Damu ya Nifasi baada ya Kujifungua.

Na tunakumbushana haya kwa sababu mbali ya kua hizi ni Damu zinazowatoka Wanawake Kimaumbile lakini pia kujua juu yake hua pia inawahusu Wanaume na Wanawake.Kwani Wanaume ndio wasimamizi wa Wake zao Mababa wa Mabinti, na miongoni mwa masuali tutakayoulizwa mbele ya Mola wetu ni **: 'Kwanini Mkeo, Binti yako hakusali katika siku kadhaa katika wakati kadhaa au kwanini Mkeo na Binti yako hakufunga siku kadhaa katika wakati kadhaa n.k.'**

Hivyo ili uweze kubeba jukumu la Qawwam – Msimamizi Kikamilifu basi ni lazima Ujue sababu zinazombatilishia Mkeo au Binti yako Udhu wake, Sala zake, Funga zake n.k.Hivyo kuna Damu za Aina tatu za Kimaumbile ziwatokazo Wanawake ambazo ni Hedhi – Damu ya Kila Mwezi kwa Mwanamke mwenye Afya. Istihadhah– Damu isiokua na Mpangilio kutokana na Matatizo ya Kiafya na Nifas ambayo ni Damu ya Uzazi.

Kwani amesema Abu Umamah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Damu ya Hedhi hua ni Nzito yenye Rangi Nyekundu ya Kiza, lakini Damu ya Istihadhah ina Rangi ya Njano na ni Nyepesi'***(Imam Al Tabarani, Imam Ad Daraqutni, na Imam Al Bayhaqi)*

Na *Aisha Radhi Allahu Anha* amesema kua: Fatima Bint Abu Hubaih alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na akamwambia: Ya Rasul Allah hakika Mimi siwezi kua Tohara Hivyo Jee Nisisali?

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia kua: Kama itakua ni Damu ya Hedhi basi hua inajulikana kutokana na Rangi yake ya Kiza na hivyo itakubidi Usisali. **Lakini kama ikiwa ina rangi nyengine basi Tia Udhu kwani hua ni kutokana Na Mrija Kutoa Damu.'** *(Sunnan An Nasai, Sunan Abu Daud)*

Ambapo Imam Al Bukhari anayo Hadith hii hii lakini ni yenye kusema kua: '**Ambapo Aisha *Radhi Allahu Anha* amesema kua:Fatima Bint Abu Hubaih *Radhi Allahu Anha* alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na akamwambia:**

يَا رَسُولَ اللَّهِ إِنِّي امْرَأَةٌ أُسْتَحَاضُ فَلاَ أَطْهُرُ أَفَأَدَعُ الصَّلاَةَ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: لاَ إِنَّمَا ذَلِكِ عِرْقٌ وَلَيْسَ بِحَيْضَةِ فَإِذَا أَقْبَلَتْ حَيْضَةُ فاترُكي الصَّلاَةَ فإِذَا ذَهَبَ قدرها فَاغْسِلِى عَنْكِ الدَّمَ وَصَلِّى

Ya Rasul Allah hakika Mimi ni Mwanamke niliejaliwa kutokwa sana na Damu hivyo siwezi kua Tohara Hivyo Jee Nisisali?

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia kua: La hio itakua ni kutokana na Mrija wa Damu na wala sio Hedhi.

Hivyo itakapoanza Hedhi basi acha Kusali na Utakapomaliza Mda wako basi jitoharishe kutokana na Damu hio kwenye Mwili wako na Sali Sala zako.'*(Sahih Bukhari)*

Naam, hizi ni baadhi ya Hadith zinazozungumzia kuhusiana na Damu za Hedhi na Istihadhah.Na jambo la kwanza tunalojifunza katika Hadith hizi ni kua Ingawa Damu hizi zinawahusu Wanawake lakini Masahabat wa Kike walikua wakimfuata *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumuulizia juu yake.

Na wala walikua hawatumii njia ya mkato labda kupitia kwa wake zake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambao walikua ni Aisha Bint Abu Bakr As Siddiq, Ummu Salamah, Ummu Habiba Bint Abu Sufyan, Zaynab Bint Jahsh, Hafsa Bint Umar Ibn Al Khattab, Juwayriyah Bint Al Harith, Safia Bint Huyay, Zaynab Bint Harith, Sawdah Bint Zamah *Radhi Allahu Anhum.*

Hivyo mbali ya kua Masahaba wa Kike *Radhi Allahu Anhum* kua na uwezo wa kumuuliza japo mmoja wa wake hao Lakini hawakufanya hivyo.

Na hadith ya kwanza tuliyoanza nayo imenukuliwa na Abu Umamah *Radhi Allahu Anhu*ambae kutokana na Jina tu basi tunaona kua ni Mwanamme na hii inatuonesha kua Somo hili linawahusu na Wanaume pia na ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akafundisha mbele ya Masahaba zake wa kiume pia.

Na hii inatuonesha kua Kiislam inakubalika kwa Mume au Baba kujua juu ya hali ya Mkewe au Binti yake kuhusiana na Hukmu hizi za Damu na hii ni kwa sababu mbali ya kua inahusiana na Mkeo au Binti yako lakini pia hua si Vizuri kwa Mkeo au Binti yako kua amuulize Mtu mwengine wa Nje ya Familia kuhusiana na mambo kama haya, hususan Mwanamme hata kama atakua ni Shaykh au ni Imam. Na ndio maana ikawa ni vizuri kwa kila Muislam kujua Juu ya haya.

Hivyo Kulingana na Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi na Salam* basi Waanzuoni wamezigawa aina hizi za Damu katika hali zifuatazo:

1-Rangi ambapo hua ni Aswad (Nyeusi) pale Hedhi Inapokua ipo kileleni kwake, kisha Ahmar(Nyekundu), kisha Ashqar (Udongo-Brown), kisha Asfar(Njano) kisha Akhdhar (Isiyokua na rangi lakini huwezi kuona upande wa pili wake).

2-Uzito ambapo Damu ya Hedhi hua nzito wakati ya Istihadhah hua Nyepesi.

3-Harufu ambapo Damu ya Hedhi hua na harufu mbaya wakati Ya Istihadhah hua haina Harufu mbaya ina harufu ya Damu ya kwaida.

4-Mgando ambapo Damu ya Hedhi hua haigandi itokapo nje lakini Damu ya Istihadhah huganda.

Kwani anasema *Al Muhaqqiq Al Faqih Al Aalamah Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadh Ahmad Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua:* '**Haina Haja ya Damu kua ni yenye Kutiririka kuhesabiwa kua ni Damu ya Hedhi, bali kama Mwanamke akiweka Kidonge cha Pamba kwenye Uke wake Na kisha baada ya kukitoa akakiona kina rangi Nyeusi, Nyekundu, Machungwa, Njano au Maziwa basi Mwanamke huyo atahesabika kua ni Mwenye Kuingia kwenye Hedhi**. **Na kama Pamba hio ikitoka ikiwa Nyeupe basi Mwanamke huyo atahesabika kua ni Tohara.'** *(Tuhfah Al Muhtaj)*

Hivyo Mwanamke atakaejikuta ana Damu basi ili ahesabike kua ameingia kwenye Siku zake anatakiwa awe ametimiza sifa zifuatazo:

1-Damu hio ni lazima Idumu kwa mda usiopungua chini ya masaa 24 Hivyo kama kutoka damu hua kunakata kata basi kukata kata kwake kunatakiwa kuwe kwa masaa 24.

2-Kipindi cha kutokaa na Damu hio kinatakiwa kisizidi siku 15, iwe kutoka huko ni kwa mfululizo au kwa kukata kata.

3-Hivyo inatakiwa kuwe na tofauti ya maaiki 15 baina ya Tohara na Kua na Hedhi.

Hivyo Mwanamke atakapokua na Damu katika hali hizi basi anatakiwa ajihesabu kua yuko katika Hedhi. Na hivyo Damu ikikata tu basi anatakiwa ajihesabie kua imeisha.

Naam.. ili kufaham zaidi basi tuangalie kulingana na mfumo wa mifano ifuatayo kama ilivyoelezewa na Al Muhaqqiq Al Faqih Al Aalamah Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadh Ahmad Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii, Imam Sulayman Ibn Umar Al Jamal Al Ajli Al Shafii na Imam Muhammad Abd Allah Al Jurdani kua:

Kwa Mfano Januari Mosi saa Nne asubuhi Mwanamke ameona Damu, ambapo tayari zimeshapita siku 15 tangu mara ya mwisho kuona Damu yake. Na hivyo basi Damu hii aliyoiona inaweza kuhesabika kua ni Hedhi kwa sababu haikuvunja Masharti tuliyoyataja.

Hivyo kutokana na Uwezekano huu basi Mwanamke huyu anatakiwa aihesabu Damu hii kama Hedhi na hivyo anatenguka Udhu na hatakiwi Kusali, wala Kufunga Na hatakiwi Kuingiliana na Mumewe, wala kusoma Qur'ani wala Kuigusa Qur'an.

Na tuseme katika ilipofika saa 12 za Jioni za Siku hio hio Ua Januari Mosi,akagundua kua Damu imesita. Hivyo akaweka Pamba na kuitoa baada 691ah ii na kugundua kua Pamba ni Safi.

Hivyo katika hali hii basi Mwanamke huyu ataihesabu Damu hio kua ni Istihadhah na wala si Hedhi kwa sababu imekata ndani ya masaa manane, wakati Damu ya Hedhi inatakiwa idumu kwa masaa 24. Hivyo katika hali kama hii basi haina haja kwake kukoga Josho kubwa.

Na kwa kua bado ni wakati wa Sala ya Magharibi basi anatakiwa asali Magharibi, na pia alipe Al Asr na Adh Dhuhr na kisha atasali Isha kwa sababu hana Hedhi. Na hivyo atafunga na kufanya yote yanayoruhuaika anapokua Tohara.

Na tuseme Damu haikutoka tena hadi siku ya Tatu ambapo akaiona tena,basi hapa ataingia kwenye Hali ya Kubatilika Udhu tena na kujizuia na kila asichotakiwa Kufanya wakati akiwa na hedhi, na hivyo hii kumaanisha kua kumbe ilikua ni Hedhi na hivyo Ibada zake zote alizozifanya hapo kabla zitakua ni Batili.

Na katika siku ya tarehe 4 Januari akaona kua Damu imekata lakini alipoweka Pamba basi Pamba hio ikawa na Rangi ya Manjano. Ambapo hii itamaanisha kua ni Hali ya Hedhi kulingana na Mtizamo Unaotegemewa wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Na katika siku ya Januari 5 akajikuta hajatoka Damu lakini Pamba imetoka na Maji kama maziwa,basi hapa pia atajihesabu kua bado yuko katika siku zake.

Na katika siku ya tarehe 6 Januari akajiona hana Damu, akaweka Pamba ambayo nayo ikawa nyeupe,basi hapa atajihesabu kua amemaliza Mzunguko wa hedhi kwa sababu siku ya kwanza alitokwa na Damu kwa Masaa manane kisha kuanzia tarehe 3 hadi 6 inakua masaa 72, kwa maana hio itakua ametokwa na Damu kwa mda wa masaa 80.

Hivyo atajitoharisha na Kuendelea na Ibada zake kama kawaida. Lakini sasa tuseme katika tarehe 10 Januari akaona tena ametokwa na Damu. Basi hapa ataingia tena kwenye hali ya Hedhi kwani alichokiona ni Damu na hivyo kumaanisha Kua na Hedhi kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii kwani Damu imetoka ndani ya siku 15. Hivyo basi kila alichokifanya katika Amali zake kitabatilika kwa sababu ya Hedhi hio.

Na ilipofika tarehe 14 akajikuta hajatoka Damu, hata baada ya kuweka Pamba, hivyo basi atajitoharisha na kua Tohara na kufanya Ibada kama kawaida. Na hakuona tena Damu hadi Febuari 1. Na hivyo kua ni mwenye kua Tohara kwa mda wa siku 15.

Hivyo basi kwa mfano kama Mwanamke huyu angeona tena Damu katika Tarehe 16 basi Damu hii isingehesabika kua ni Hedhi kwa sababu Mzunguko wake wa Hedhi Umeshamalizika.

Na hivyo Damu hio inahesabika kua ni tatizo la Damu ya Istihadhah.'*(Tuhfah Al Muhtaj- Imam Ibn Hajar Al Hatami, Hashiyat Al Jamal ala Fat-h Al Wahhab bi Sharh Minhaj Al Tulab– Imam Sulayman Al Jamal, Fat-h al Aalam Bi Sharh Murshid Al Anam- Imam Muhammad Abd Allah Al Jurdani)*

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari kua: '**Inatakiwa ifahamike kua Mda mdogo kabisa wa Kutokwa na Damu ya Hedhi hua ni Mchana mmoja na Usiku mmoja yaani Masaa 24.'***(Asna Matalib)*

Kwa maana hio basi kama Damu ikitoka kwa kipindi kifupi zaidi ya hicho basi hio haiwi Hedhi bali hua Istihadhah. Ambapo utokaji huo wa Damu ya Hedhi unaweza kutokea aidha katika hali ya Muttasil yaani Mfululizo au kwa hali ya Mutaqatti au Mutafarriq yaani kwa kukatika katika.Na inaweza kuchukua Mda wa siku 15 ambazo ndio siku za Urefu wa Hedhi, na kutoka kwake hua ni katika kipindi cha Hedhi

Na imesemwa katika Tuhfah Al Aiza kua: '**Mkatiko katiko wa Hedhi hua ni pale Damu itakapotoka kwa masaa machache ikasita na kisha ikatoka tena, na baadhi ya Wakati ikakata Kwa siku kadhaa ndani ya siku 15. Hivyo ni Muhimu kuhesabu mda wa kutoka Damu, kwani kama ikiwa ni zaidi ya masaa 24 basi hio itakua Hedhi hata kama hali hio itatokea katika siku ya 15**. **Na Hivyo kama Damu hio itatoka kwa mda usiofikia masaa 24 basi hio itakua ni Istihadhah.'***(Tuhfah Al Aiza)*

Hivyo Damu itakapotoka basi Mwanamke anabatilika Udhu wake na anatakiwa kutofanya yote yaliyokatazwa wakati akiwa ndani ya Hedhi, hadi pale atakapohakikisha kua Hio iliyomtoka si Hedhi, kisha hapo ndio itambidi Alipe Ibada zake, na kama Damu haikua nyingi basi Atajisafisha na Kutia Udhu na Kusali.

Na anasema Al Muhaqqiq Al Faqih Al Aalamah Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadh Ahmad Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: '**Damu ndani ya Uke hua inahesabiwa kua ni Hedhi kama ikiwa ipo katika Wakati wa Hedhi**. **Hivyo Hukmu ya Mwanamke kua ana Hedhi na Hukmu zinazofuatia kutokana na kua na Hedhi hio hua zinategemeana na Kujua kama ipo Damu hio ndani ya Uke ambayo inaweza kua ni ya Hedhi**. **Hivyo kama itakua ipo basi Damu hio itakua ni ya Hedhi, na kama hakuna basi si hedhiKwa sababu Hedhi hua inakuja na kutoka, hivyo ikiwa kuna Damu ndani ya Uke basi hua inahesabiwa kua ni Hedhi hata kama Damu hio haikutoka nje.'***(Fatawa Al Fiqhiyyah Al Kubra)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Buhuti Al Hanbal basi yeye anasema kua: '**Kile kinachothibitishwa kutoka nje**. **Hua pia kinahisikana ndani ya Uke, hivyo kama Mwanamke akihisi Hedhi kabla ya**

kuzama Jua wakati akiwa amefunga, basi funga yake hio hubatilika hata kama Damu hio itakua haijatoka nje hadi baada ya kuzama kwa Jua.'*(Muntaha Al Irada)*

Ambapo kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: '**Dharurah ya Damu ya Hedhi humaanisha Damu kuanzia ndani Kutoka nje ya Uke, kwa sababu Hedhi, Nifas na Istihadhah hua hazithibitishiki vyenginevyo isipokua hivyo katika kutoka nje kwake na kuonekana.**'*(Badai Sanai)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- ISTIHADHAH

❖❖❖❖

Damu ya Istihadhah hua ni Damu ambayo aidha hutoka kwa mfululizo au bila ya kua na mpangilio katika wakati ambao si wa Mzunguko wa Damu ya Hedhi wala ya Nifasi. Hivyo Kishariah basi Istihadhah hua ni Damu inayotoka kutokana na matatizo ya Kiafya kupitia katika Mrija wa Damu uliop mwishoni mwa Uke ambao huaunajulikana kama Adhil. Hivyo Damu ya Istihadhah hutokea kulingana na Dalili zifuatazo:

Kutokwa na Damu mara mbili katika Siku tofauti ndani ya Siku zisizozidi siku 15.

Kutokwa Na Damu baada ya Kupitiliza Siku 15 au zaidi.

Kutokwa na Damu kwa usiozidi Masaa 24.

Kutokwa na Damu kabla ya Kutimiza Miaka 9.

Kutokwa na Damu baada ya kumaliza Siku 60 za kipindi cha Nifasi.

Na kwa upande wa Kisayansi basi tunaona kua Istihadhah hua Utokwaji wa Damu wa Mwanamke katika Uke wake katika kipindi cha nje ya wakati wa Hedhi.

Ambapo Damu hii hua ni yenye kutoka kwenye Viungo vya Fuko la Uzazi na wal si kwenye Kibofu cha Mkojo wala kujeruhika kwa Sehemu za siri.Na kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Istihadhah hua ni Jeraha katika Mshipa wa Damu, kwani Istihadhah hutokana na Jeraha au Ugonjwa kwenye Mshipa wa Damu unaopita Chini ya Fuko la uzazi.Hivyo Istihadhah hua si Ugonjwa bali hua ni Dalili inayoonesha kua Kuna Tatizo katika Kizazi cha Mwanamke husika.

Ambapo Tatizo hilo linaweza kua linatokana na Kupungua kwa Nguvu ya Mfumo wa uzalishaji wa kemikali za Mwilini, Au Kwenye Mfuko wa Mayai, au Mwanamke kua na Mayoma au Madonge ya Nyama Nyama kwenye Kizazi, Kunenepa kwa Ukuta wa Kizazi au Kutokana na Madhara ya baadhi ya Dawa za Uzazi wa Mpango kutoendana na Mwanamke husika, au Maradhi ya Uasharati, au Saratani, Kuzidi kwa Uzito wa Mwili,Kua na Msongo wa Mawazo, na baadhi ya wakati hua ni kutokana na kupandikizwa kifaa cha Kuzuia utungaji Mimba ndani ya Fuko la Uzazi n.k.

Ambapo imesemwa kwenye Tuhfa Al Aizza kua: **'Kama ikiwa Damu itamtoka Mwanamke kwenye sehemu zake za Siri baada ya Matumizi ya Dawa au Kuwekewa Kitu, jambo ambalo hua ni kawaida kwa Wanawake, basi Hukmu yake ni kua itahesabiwa kua ni Hedhi kwa masharti ya kua haitopitiliza kile kipindi cha Hedhi. Hivyo kama ikipitiliza kipindi cha Hedhi basi Damu Hio haitohesabiwa kua Ni Hedhi bali itahesabiwa kua ni Istihadhah, na hii ni kwa sababu ya matumizi**

ya Dawa anazotumia. Hivyo Damu itakamtoka katika kipindi cha mwanzoni itahesabika kua n Hedhi lakini itakayofuata itahesabiwa kua ni Istihadhah ambayo ni Damu safi.'*(TuhfahAl Aizza)*

Hivyo kuhusiana na hukmu yake Mwanamke mwenye Istihadhahanasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyah Sharab Ibn Yahya An Nawawi Al Shafii kua: '**Mwanamke Mwenye Istihadhah hua ni mwenye kushikamana na Hukmu ya kua ni Tohara kulingana na Hukmu za Sala, Saumu, Itiqaf, Kusoma Qur'an n.k.'** *(Al Majmuu)*

Na akasema tena Imam An Nawawi kua: '**Hukmu ya Mustahadah au Mwanamke mwenye Istihadhah hua ni sawa na Hukmu ya Mtu mwenye Matatizo ya Mkojo kutoka bila kizuiziJambo ambalo hua halimzuii Kusali wala Kufunga, hivyo hua ni Wajib kwa Mwanamke mwenye Tatizo la Mkojo (au Istihadhah) kukosha Uke wake na kisha Kuuziba kwa Kitambaa (au Pad)**. **Na kisha anatia Udhu na Kusali haraka sana bila kupoteza mda**. **Na hata kama Mda ukipotea tuseme kwa Kujianda kuvaa mavazi ya Sala,au kusubiri Jamaa n.k, basi hii hua haina Tatizo kwani Udhu wake hautobatilika.**

Lakini Hata hivyo kama atapoteza mda kwa mambo yasiyokua Muhimu, basi Udhu wake utabatilika na hii ni kutokana na Mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii. **Hivyo hua ni Wajibu kwa Mtu Mwenye Istihadhah kujitoharisha na kutia Udhu katika kila wakati anaotaka Kusali.'***(Minhaj Talibin)*

Na hii ni kutokana na Hadith iliyomo katika kitabu cha Sunnan Abu Daud ambayo inasema:

عن حَمْنَةَ بِنتِ جَحشٍ، قالتْ: كُنتُ أُستَحاضُ حَيضةً كثيرةً شديدةً، فأَتَيْتُ رسولَ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم أَستَفتيهِ وأُخبِرُه، فوجَدْتُه في بَيتِ أُختي زينبَ بنتِ جَحشٍ، فقُلْتُ: يا رسولَ اللهِ، إنِّي امرأةٌ أُستَحاضُ حَيضةً كثيرةً شديدةً، فما تَرى فيها؟ قد مَنَعَتْني الصَّلاةَ والصَّوْمَ، قال: أَنعَتُ لكِ الكُرْسُفَ؛ فإنَّه يُذهِبُ الدَّمَ، قالتْ: هو أَكثَرُ مِن ذلكَ، قال: فاتَّخِذي ثَوبًا

Amesema Hamnah Bint Jahsh *Radhi Allahu Anha* kua: 'Isihadhdhah yangu ilikua ni yenye kutoka kwa wingi sana Damu yake, hivyo ni kaenda kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kuomba ushauri. Nami nikamkuta katika nyumba ya Dada yangu ambae ni Zaynab Bint Jahsh *Radhi Allahu Anha,* na nikasema: 'Ya Rasul Allah! hakika mimi ni Mwanamke mwenye kutokwa sana na Damu ya Hedhi, hivyo Jee unafikiraje? Jee imenizuia mimi Kufunga na Kusali?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Nakushauri kua utumie Pamba, kwani hua inanyoya Damu' ambapo Hamnah *Radhi Allahu Anha* akasema: 'Haitoshelezi kwa hilo''**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Basi Tumia Kitambaa'(Sunnan Abu Daud)*

Naam, hivyo kabla ya kuendelea basi tunafahamishana kua tunaona kua Imam An Nawawi katika Fatwa yake hii amesema kua Hukm ya Mwanamke mwenye Istihadhah hua ni sawa na Hukmu ya Mtu mwenye matatizo ya kutozuilika kwa Mkojo. Na bila ya shaka basi Tatizo la kutozuilika kwa mkojo hua ni la watu wote yaani hua ni tatizo la Wanaume na la Wanawake pia. Hivyo basi juu ya hili pia tunaona kua Hukmu yae ni moja kwa Wanawake na Wanaume, yaani tatizo la kutozuilika kwa mkjo kwa Mwanamme basi Hukmu yake hua sawa na hukmu ya mwanamke mwenye Isitadhah.

Hii nimegusia tu Kuonesha Umuhimu wa kuyajua yote haya na namna yanavyoingiliana kihukmu kwa Wanaume na Wanawake na tutafafanua zaidi baadae Inshaa Allah.

Na pia katika fatwa hii ya Imam An Nawawi imeruhusu kwa Mtu mwenye Tatizo la Istihadhah au la Mkojo kua ni mwenye kusubiri Jamaa.

Ambapo anasema Imam An Nawawi kua: '**Mwanamke Maamuma anaruhusika Kusali Pembeni ya Mwanamke mwenye Istihadhah au mwenye Tatizo la Kutozuilika kwa Mkojo na Sala yao itakua Sahih.Lakini kwa Mwanammke Maamuma hua haruhusiki kusali Pembeni ya Mwanamke Mutahayyarah(yaani Mwanamke asiekua na Uhakika kuhusiana na Tohara yake kutokana na kusahau kwake kama ilivyosemwa katika Al Majmuu) na huo ndio Mtizamo Sahih wa Madhhab ya Imam Al Shafi**i.*'(Rawdha Talibin)*

Na hii ni kwa sababu Mwanammke Mutahayyarah hua haruhusiki kua Imam hata kama Maamuma wake nae atakua Mutahayyarah kama yeye.'*(Nihayat Al Muhtaj, Tuhfah Al Muhtaj)*

Ambapo *Imam Al Muhaqqiqin Al Alamah Al Faqih* Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii anafafanua zaidi suali hili kwa kusema: '**Mwanamke anaesali na Mustahadhah (Mwanamke mwenye Istihadhah) hua ni Sahih kwa sababu Sala ya Mustahadhah hua Sahih Hivyo kama Maamuma akiwa pia Mustahadhah basi Sala yao ya Jamaa hio itakua Sahih bila ya kuwepo kwa Mipingano ya Wanazuoni juu ya Jambo hilo.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Hivyo Mwanamke mwenye Istihadhah anaweza kusali Sala ya Jamaa iwe kama yeye atakua ni Imam wa Wanawake wenzake au Maamuma.

Ambapo Ili Sala yake iwe Sahih basi lazima Kutimiza Masharti tuliyotaja ambayo ni:

1-Kujitoharisha Uke wake.

2-Kubadilisha Kitambaa atakachotumia Kujizibia Uke wake katika kila Wakati anaotaka Kusali.

3-Kujitayarisha hivyo na kutia Udhu mara tu kabla ya Kutaka Kusali.

4-Kuharakisha Kusali isipokua labda kama itakua anavaa nguo za Sala au anasubiri Jamaa.

Ambapo Masharti haya hua pia kwa Mtu mwenye Matatizo ya Kutokwa na Mkojo bila Kizuizi iwe mtu huyo ni Mwanamke au Mwanamme

Hivyo Wanazuoni wanakubaliana kua Mwanamke mwenye Istihadha hua anatakiwa Awe ni mwenye kutia Udhu katika kila wakati anaotaka Kusali. Na hivyo pia Wanakubaliana pia kua Udhu wa Mwanamke husika hua unabatilika mara tu baada ya Kumalizika Sala ya Wakati wa kipindi husika.Yaani kama ametia Udhu kwa ajili ya Sala Al Dhuhr basi Ikimalizika Salat Al Dhuhr na Sunna zake basi na Udhu wake unabatilika hivyo ukifika wakati wa Al Asr itambidi Atie Udhu Upya.

Ambapo kwa upande wa Imam Urwa Ibn Al Zubayr, Imam Sufian Al Thawri, Imam Abu Thauri basi wao wanasema kua: **'Hairuhusiki Kwa Mwanammke mwenye Istihadhah kusali Sala zaidi ya Moja katika kika kimoja.'**

Hivyo Mwanamke mwenye Istihadhah hashurutiki kukoga josho kubwa kama la Hedhi au Nifasi kila pale wanapotaka kusali, ambapo huo ni Mtizamo wa Masahaba kama Ali Ibn Ab Talib, Abd Allah Ibn Masud, Abd Allah Ibn Abbas, Aisha *Radhi Allahu Anhum.*Na pia ndio Mtizamo wa Maimamu kama Imam Urwah Ibn Al Zubayr, Imam Abu Salamah bn Abd Rahman, Imam Abu Hanifa, Imam Malik Ibn Anas, Imam Muhammad Idris Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal ambapo wote wanakubaliana juu ya hilo. Ambapo anasema Imam Al Shafii kua:

'*Rasul Allah Salallahu Alayh wa Salam* alimwambia Um Habibah kua akoge nakisha asali, na haikuelzewa kwenye hadith kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuamrisha Ummu Habibah *Radhi Allahu Anha* kua akoge katika kabla ya kila wakati anaotaka kusali, hivyo Kuoga huko kulikua ni kwa hiari na wala si kwa kulazimisha.'

Ambapo hukumu hizi pia ni kwa Mtu mwenye tatizo la Kutozuilika kwa Mkojo iwe Mtu huyo ni Mwanamke au Mwanamme.

Na Ingawa Imam Ibn Jarir At Tabari anasema kua: '**Wanazuoni wanakubaliana kua Mwanamke mwenye Istihadhah hua anaruhusika Kusoma Qur'an.'**

Na kwa Upande wa Imam Ibrahim An Nakhai na Imam Abu Hanifa kua na Mtizamo usemao kua: '**Mwanamke Mwenye Istihadhah hua haruhusiki Kuugusa Msahafu na wala Kugusa kitu chochote chenye Aya Kamili ya Qur'an.'**

Lakini Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anasema kua: **'Mwanamke mwenye Istihadhah anaruhusika Kusoma Qur'an kama akitia Udhu na anaruhusika Kuigusa Qur'an na Kuibeba pia, na anaruhusika Kusujudu Sijdat Tilawat na Sijdat Shukr.**

Na ni Lazima Asali, Afunge na afanye kila kitendo ambacho kinahesabia kua ni Ibada ambacho kinafanywa na Mtu aliekua Tohara.

Na hakuna kutofautiana juu ya hili miongoni mwetu katika Madhhab yetu na As-hab Al Wujuh wetu wamesema kua: Kauli inayokubalika juu ya Mwanamke mwenye Istihadhah ni kua Hahusiani na Hukmu yeyote ya Hedhi, na juu ya hili hakuna kutokubaliana Juu yake.

Na Imam Ibn Jarir amesema kua kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua Mwanamke mwenye Istihadhah anaruhusika kusoma Qur'an na ni lazima kwake kufanya yale yote yanayofanywa na Mtu alie Tohara.'*(Al Majmuu sharh Al Muhadhdhab)*

Ambapo juu ya Makubaliano hayo ya Wanazuoni basi yamenukuliwa pia na Mujtahid Imam Abu Bakr Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii, Imam Al Marghinani na Imam Al Ayni.

Na bila ya shaka hua inaruhusika kwa Mwanamke mwenye Istihadhah kuingiliana na Mumewe na hii ni kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Malik, Madhhab ya Imam Al Shafii na kuna Kauli moja kwa Upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Kwani kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi mtizamo wao ni kama unavyoelezewa na Al Aalama Ibn Qasim Al Hanbal pale aliposema kua: '**Mwanamke mwenye *Istihadhah* hua haruhusiki kuingiliwa isipokua pale itakapokua kuna khofu ya Uzito kwa upande wa Mume au wa Mke.**

Na hii ni kulingana na Mtizamo wa Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua: Mwanamke mwenye Istihadha hua hatakiwi kuingiliwa na Mumewe ila kama ikiwa kuna Khofu kwa Mume au kwa Mke basi hua Inaruhusika, na pia inaruhusika kama ikiwa mmoja wao ana hamu sana ya mwenzake.

Na pia Kuna Mtizamo unaoruhusu kumuingilia Mwanamke mwenye Istihadhah ambao huu ndio Mtizamo unaokubalika na Wanazuoni wengi sana.

Na hii ni Kutokana na Hadith ya Hamnah *Radhi Allahu Anha* ambae alikua na Istihadhah ya mda mrefu na Mumewe ambae ni Talha *Radhi Allahu Anhu* alikua akiingiliana nae na vile Umm Habibah *Radhi Allahu Anha,* ambapo Hadith zote hizi zimenukuliwa na Imam Abu Daud.

Hivyo Mwanamke mwenye Istihadhah hua kwa kila hali si sawa na Mwanammke mwenye Hedhi na *Allah Subhanah wa Taala a*metofautisha baina ya Hedhi na Istihadhah Kwani Hedhi hua inachukua Mda mrefu na ina Madhara zaid kuliko Istihadhah.

Wakati Istihadhah ni Damu inayotoka kwenye Mrija wa Damu kutoka ndani ya Uke kama vile itokavyo Damu ya Pua.

Na utokaji wake hua una madhara na usitaji wake unathibitisha Afya ya Mwanamke, wakati Hedhi hua ni kinyume chake na Asili zake, hukmu zake na sababu zake zinatofautiana.

An Nawawi amesema kua: Inaruhusika Kuingiliana katika wakati ambao unahesabika kua ni Tohara na wala haikirihishi, hata kama Damu itakua inatoka,na huo ndio Mtzamo wetu na wa wengi miongoni mwa Wanazuoni.

Na hakuna Hukmu ya Hedhi inayoweza kuthibitishwa kuhukumiwa katika Istihadhah.

Ibn Jarir amesema kua Kuna Makubaliano ya Kua mwenye Istihadhah anaruhusika Kusoma Quran na kufanya yale ayafanyayo mwenye Tohara, kwa sababu hua ni sawa na Mtu mwenye Tohara katika Sala na Funga na ndio pia katika Kuingiliana.

Na Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* amesema kua Mwanamke mwenye Istihadhah anaruhusika kuingiliana na Mumewe. *(Rawdhah Al Murabbah)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- NIFAS

❖❖❖❖

حَدَّثَنَا نَصْرُ بْنُ عَلِيٍّ الْجَهْضَمِيُّ حَدَّثَنَا شُجَاعُ بْنُ الْوَلِيدِ عَنْ عَلِيِّ بْنِ عَبْدِ الْأَعْلَى عَنْ أَبِي سَهْلٍ عَنْ مُسَّةَ الْأَزْدِيَّةِ عَنْ أُمِّ سَلَمَةَ قَالَتْكَانَتْ النُّفَسَاءُ عَلَى عَهْدِ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم تَجْلِسُ أَرْبَعِينَ يَوْمًا وَكُنَّا نَطْلِي وُجُوهَنَا بِالْوَرْسِ مِنْ الْكَلَفِ

Amesema Nasr Ibn Jahdhami kua amesema Shujaa Ibn Walid Ahu Badr kua amesema Ali Ibn Abd Al Aala kua amesema Abu Sahl kua amesema Masa Al Azdiyah kua amesema Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* kua:

Mwanamke aliejifungua Mtoto alikua akikaa Siku 40 katika Kipindi cha wakati wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Na tulikua Tukipaka Dawa Nyuso zetu kwa ajili ya Kuficha mabaka yanayotokea Usoni'*(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhii, Imam Ibn Majah na Musnad Imam Ahmad)*

Naam Hadith zinatuonesha namna *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyokua akiufundisha Ummah wake kila kitu kuhusiana na Afya zao Kidunia na Kiakhera.

Kiasi ya kua alikua akiwafundisha Wanawake nini cha Kufanya pale wanapokua kwenye Hedhi, Istihadhah na Nifasi pia kama tulivyoona hapo kabla na katika Hadith hii pia ambayo ndani yake tunaona kua mmoja katika Wake zake *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* aitwae Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* anasema kwa kumaanisha kua:

Wanawake walikua wakibakia katika hali ya Nifas kwa mda wa siku 40 na hivyo hawafungi wala hawasali hadi watimize Siku 40, isipokua labda kama atakua Tohara kwa kukatika kwa Damu hio kabla ya kutimia siku hizo

Na hivyo kutokana na Kujifungua huko na kukaa ndani basiNyuso zao zilikua zinafanya Mabaka Mekundu na meusi na hivyo ilikua ikiwabidi kujipaka Dawa ya Unga utokanao na Mmea wenye Rangi ya Manjano yaani kama Liwa.

Na anasema Imam Abu Isa Al Tirmidhii kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hii ni Hadith yenye upekee ambao sisi hatujwahi kuusikia isipokua kutoka kwenye Hadith ya Abu Sahl kupitia kwa Musa Al Azdiyyah kutoka kwa Ummu Ul Muuminina Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha.'***(Sharh Jamii Tirmidhi)*

Ambapo Jina halisi la Abu Sahl ni Kathir Ibn Ziyad. Na amesema Imam Muhammad Ibn Ismail Al Bukhari kuhusiana na Abu Sahl kua: **'Ali Ibn Abd Al Alaa ni Mwenye Kuaminika katika Hadith na Abu Sahl pia ni mwenye kuaminika katika Hadith'***(Sharh Jamii Tirmidhi)*

Ambapo kutokana na Hadith hii basi Wanazuoni wa Masahaba *Radhi Allahu Anhum*, Wanazuoni wa Tabiina na Tabii Tabiina wanakubaliana kua **: 'Mwanamke aliejifungua hua hatakiwi Kusali hadi baada ya siku 40. Isipokua pale Damu ya Nifas itakapokua imekata kabla ya siku hizo, basi atajitoharisha na kuanza Kusali kama Kawaida na kufanya mambo mengine yote anayoruhusika kufanya Mwanamke aliekua Tohara.**

Na kama ikiwa amepitiliza Siku 40 na Damu inaendelea kutoka, basi hapa Damu hio haitohesabika kua ni Nifas na hivyo atajitoharisha na kuendelea na Ibada zake kama ilivyokua kwenye Istihaadhah.

Ambapo huu ndio Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni akiwemo Imam Sufyan Ath Thawrh, Imam Abd Allah Ibn Mubarak, Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, na Imam Is-haq Ibn Rahawayh.

Na kwa upande wa Imam Hasan Al Basr basi yeye amesema kua: 'Haruhusiki Mwanamke kusali hata kwa siku 50 kama hajawa Tohara kutokana na Nifas.'

Ambapo kwa Upande wa Imam Ataa Ibn Abi Rabah na Imam Abd Rahman Ash Shaabi basi wao Wanasema kua Hairuhusiki kwa Mwanamke Kusali hata kama ikiwa ni Siku 60 kama ikiwa haijakata Damu ya Nifas na kua Tohara.'*(Sharh Jamii Tirmidhii)*

Naam..huo ni Mtizamo wa kwanza kuhusiana na Hadith hii. Nami nimeichagua makusudi hadith hii kwani kusema kweli ni kua hii ni hadith nzuri sana kwa wale wanatoka kufahamu kwanini Wanazuoni wakatofautiana pale tunapozungumzia kuhusiana na Ilm ya Hadith na pia kutofautina kwa Mitizamo ya Fiqh ya Madhhab tofauti.

Hivyo kama tutakua makini basi ndani yake In-shaa Allah tutajifunza mengi sana mbali ya kutenguka kwa Udhu kutokana na Nifas.

Hivyo kama tulivyoona kua kulingana na Mtizamo wa Imam Al Bukhari na Imam Yahya Ibn MaiAin kama alivyosema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani ambae anaendelea kusema pia kua: **'Hadith hii imenukuliwa na Ahmad Ibn Hanbal, Abu Daud, Al Tirmidhii, Ibn Majah, Al Daraqutni na Imam Al Hakim.'**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Hibban basi yeye anasema kua Abu Sahl ni Dhaif, mbali ya kua ni mwenye kuaminika katika Hadith na Imam Al Bukhari na Ibn MaAin.

Na Imam Ad Daraqutni amesema kua Hadith hii haiwezi kutumika kama Uthibitisho, na Imam Ibn Qatan akasema kua Darja yake Hadith hii haijulikani na Imedhoofishwa na Kathir Ibn Zaid.

Na amesema Imam An Nawawi kua: Kauli ya Wanazuoni wa Fiqh kuhusiana na Hadith hii kua ni Dhaif na haikubaliki. Na inauthibitisho unaoipa nguvu utokao kwa Imam Ibn Majah ambae yeye ameinukuu kutoka kwa Salam kupitia kwa Humayd kupitia kwa Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:

أن رسول الله صلى الله عليه وسلم وقت للنفساء أربعين يوماً، إلا أن ترى الطهر قبل ذلك

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameweka mda wa siku 40 kwa Mwanamke aliejifungua, isipokua pale atakapopata Tohara kabla yake siku hizo. Ambapo hakuna alieinukuu hadith hii kutoka kaa Humayd isipokua Salam ambae nae ni dhaifu.**

Lakini Abd Razaq ameinikuu Hadith hii kupitia katika Sanad (mnyororo wa walionukuu) nyengine iliyotoka kwa *Anas Radhi Allahu Anhu* hadi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.

Na pia Imam Al Hakim amenukuu Hadith nyengineyo kutoka kwa Al Hasan kupitia kwa Uthman Ibn Abi Al Aas *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:

وقت رسول الله صلى الله عليه وسلم للنساء في نفاسهن أربعين يوماً

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*: 'Ameweka Mda wa Mwanamke aliejifungua wa Nifas kua ni Siku 40.**

Na Imam Al Hakim akasema kua Hii ni Hadith Sahih kama imepitia kwa Abu Hilal' *(Talhis Al Khabir)*

Baada ya kusema hivyo kuhisiana nayo hadith hii katika Talkhis basi Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii akasema katika Bulugh Al Marami kua: **'Al Hakim ameikubali hadith hii na kusema kua ni Sahih na wala hakuikosoa.'***(Bulugh Al Marami)*

Na kisha pia Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii akasema katika Al Taqrib Al Tahdhib katika Historia ya Masa Al Azdiyyah kua: **'Na kama mnavyojua kua hii Ni Hadith inayokubalika.'***(Al Taqrib wa Al Tahdhib)*

Ambapo Masa Al Azdiyyah ni Mwanazuoni wa Kike wa Ilm Al Hadith ambae amewasomesha kina Imam Kathir Ibn Ziyad, Imam Al Hakam Ibn Utaybah, Imam Zaid Ibn Ali Ibn Husein na Imam Muhammad Ibn Ubaid Allah Al Azrami Na kwa upande wa Imam Al Bukhari basi alikua ni mwenye kusifu Usahih wa Hadith zake na pia Imam Al Hakim amesema kuhusiana na Usahih wa Hadith hii kutoka kwake.

Hivyo basi ingawa hadith hii imezungumziwa katika Mitizamo tofauti na Wanazuoni wa Hadith lakini haya hivyo inaungwa Mkono kiuthibitisho na hivyo kua ni yenye kutegemewa na Wanazuoni pale tunapozungumzia kuhusiana na Hukmu ya Damu ya Nifasi kua ni siku 40.

Ambapo huu ndio Mtizamo unaotegemewa na Wengi Miongoni mwa Wanazuoni.Hivyo Mwanamke aliejifungua basi hua anatakiwa akae siku 40 bila ya kufanya Ibada anazotakiwa kufanya Mwanamke aliekua Tohara kama kufunga, Kusali, Kuingiliana na Mumewe,n.k. Isipokua kama Damu itakata kutoka kabla ya Kumalizika siku 40, basi itambidi ajitoharishe na hapo ataruhusika kusali, kufunga n.k.

Na kama Damu itarudia tena kutoka ndani ya Siku 40 basi itambidi asite Kufanya Ibada zote anazoruhusika kufanya wakati akiwa Tohara. Na kisha baada ya Siku 40 atajitoharisha na kuendelea na Ibada kama kawaida. Kama Damu ikitoka baada ya Siku 40 basi na aiangalie kama ni ya Hedhi au ni ya Istihadhah na kisha achukue hatua kulingana na Hali husika.

Kwani anasema Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qalyubi Al Masri Al Shafii kua: '**Nifasi hua ni Damu ambayo hutoka baada ya Fuko la Uzazi kua Huru kutokana na Mtoto au hata Alaqah (Pande La Damu) au Mudghah (Pande la Nyama) na pia kabla ya Kufikia Mda wa Tohara baada ya Kujifungua ambapo Mda wake hua ni siku 15**. **Hivyo Kama Mtu akiona Damu baada ya Siku ya 15 na zaidi baada ya Kujifungua basi hio haito hesabika kua ni Nifasi.'***(Hashiyah Al Qalyubi)*

Na akasema Imam Al Muhaqqiqin Al Aalamah Al Faqih Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: '**Nifas hua Ni damu inayotoka baada ya Fuko la Uzazi kua huru kutokana na Mtoto hata kama ikiwa ni katika hali ya Al Alaqah, au Mudghah na kabla ya kipindi cha Tohara baada ya Kujifungua ambacho ni Siku 15**. **Hivyo Kama Mtu akiona Damu baada ya siku ya 15 baada ya kujifungua basi hio hua ni Hedh**i.'*(Tuhfah Al Muhtaj)*

Imam Al Muhaqqiqin Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Hakuna kipindi cha Mda mfupi cha Nifasi, yaani kwa maana nyengine basi ni kwamba Nifas hua haipimiki kwani huonekana kulingana na inavyotoka, hata kama itakua ni kidogo ambapo kwa makisio tunaweza kuhesabia udogo kua ni wa sekunde moja na ingawa ukubwa wa Nifas Hua ni siku 60 lakini kwa kawaida hua ni siku 40, haya ni majibu yaliyopatikana kutokana na Istiqra -Utafiti kama ilivyoSemw**a.'*(Tuhfah Al Muhtaj)*

Kwa maana hio basi Nifasi hua ni Damu ambayo inatoka kwa sekunde tu baada ya kujifungua, au itatoka kwa mda wa siku 40 au siku 60. Na hutoka aidha kabla ya Kujifungua katika kujifungua au ndani ya Siku 15 baada ya Kujifungua. Hivyo kama Mtu akiona Damu baada ya kupita siku 15 basi hio inayotoka itahesabika Kua ni Hedhi.

Na pia kama Damu itaendelea kutoka kwa zaidi ya siku 60 basi hua kuna haja ya kuifuatilia Damu hio kwani kama itakua inatoka kwa mfululizo bila kusita hata kwa sekunde basi Damu hio itakua ni Istihadhah. **Na kama itakua inasita sita na kuendelea basi itakua ni Hedhi**.*(Al Ibanah Wa Al Ifadhah)*

Naam..hio ni kuhusiana na Mtoto ambapp kuhusiana na atakaepukutisha Mimba basi amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Mwanamke atakaepukutisha Mimba ikatoka katika hali ya Aalaqah - Pande la Damu, au Mudghah Pande la Nyama basi wajibu wa Kujitohariaha kwa kukoga kuna mitizamo miwili juu yake baina ya As-hab Al Wujuh wetu Ambapo Mtizamo unaokubalika zaidi ni Kua Kujitoharisha kwa kukoga hua ni Wajibu.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na akasema tena Shaykh Ul Islami Imm An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Nifas basi iwe Mtoto amezaliwa akiwa Mkamilifu ama la, iwe yuko Hai ama la, Iwe Mimba Imepukutika na Kutoa Pande la Damu Au Nyama, na Mkunga akathbitisha kwa kusema kua "Huu ndio mwanzo wa Maumbile ya Ibn Dam" basi Damu itakayofuatia hapo hua ni Nifa**s.'*(Rawdha Talibin)*

Kwa maana hio basi hapa kuna hali zifuatazo:

1-Kama Damu itatoka katika wakati ambao si wa Tohara, na ikahesabiwa kua haikutokana na Upukutishwaji wa Mimba, basi Damu hio itahesabiwa kua ni Hedhi na pia kama Damu ikitoka kabla kupukutika kaa Mimba huhesabika kua ni Hedhi.

2-Kama Damu itatoka katika Kipindi cha Tohara au haitimizi mzunguko wa masaa 24 au kuendelea kutoka kwa mda wa zaidi ya siku 15 na ikithibitishwa kua si kutokana na kupukutika Kwa Mimba basi Damu hi itakua ni Istihadhah.

3-Kama Damu itatoka katika wakati ambao si wa Tohara na ikathibitishwa kua ni kutokana na pukutisho la Mimba wakati ikiwa katika hali ya Alaqah yaani Pande la Damu basi Damu hio hua ni *Wiladah*.

Ambapo Wiladah hua ni Kujifungua bila kutokwa na Damu na hivyo Mwanamke husika Humbidi kukoga Janaba badala yake na hii ni kwa sababu Mtoto hutokana na Manii ya Mwanamme na Mwanamke. Na hivyo Hukmu yake hali hii hua ni Kujitoharisha kwa kukoga ingawa njia Damu haikutoka katika wakati alipozaliwa Mtoto au Pande la Damu au Pande la Nyama kama alivyosema Imam An Nawawi.

4-Kama ikiwa Damu itatoka katika wakati ambao si wa Tohara na ikathibitishwa kua ni kutokana na Upukutishwaji wa Mimba katika wakati wa hali ya Pande la Damu au Pande la Nyama basi kitakachofuatia hua ni Nifas.

Na amesema Umm Salamah R*adhi Allahu Anha* katika hadith isemayo kua:

عَنْ كَثِيرِ بن زِيَاد، قال: حدثتني الأَزْدِيَّة يعني مُسَّةَ قالت: حَجَجْتُ فَدَخَلْتُ عَلَى أُمِّ سَلَمَةَ فَقُلْتُ: يَا أُمَّ المؤْمِنِين، إِنَّ سَمُرَةَ بن جندب يَأْمُرُ النِّسَاءَ يَقْضِينَ صَلَاةَ الْمَحِيضِ فَقَالَتْ: «لَا يَقْضِينَ كَانَتِ

المرْأَةُ من نِسَاءِ النبي صلى الله عليه وسلم تَقْعُدُ فِي النِّفَاسِ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً لَا يَأْمُرُهَا النبي صلى الله عليه وسلم بِقَضَاءِ صَلَاةِ النِّفَاسِ»

Kwani anasema Anasema Kathir Ibn Ziyad kua : **Ameniambia Mimi Al Azdiyatt yaani Musa kua: 'Nilifanya Ibada ya Hija na kisha nikamtembelea Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* na kumwambia:** '**Ewe Mama wa Waislam, Samura Ibn Jundub anawaamrisha Wanawake Kulipa Sala zao ambazo hawakuzisali walipokua na Nifasi.**

Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* akasema: Hawatakiwi Kulipa, kwani Mwanamke miongoni mwa Wake wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angebakia katika Hali ya Nifasi kwa muda wa usiku wa siku 40 bila ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumuamrisha kua alipe Sala za siku hizo 40.'*(Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhii, Imam Ad Darimi na Imam Ahmad Ibn Hanbal)*

Naam hii ni Hadith ambayo Mama wa Waislam yaani Mke wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam:* Aitwae Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha*akitoa Fatwa baada ya kusikia kua Samura Ibn Jundub anawalazimisha Wanawake waliomaliza kipindi cha Nifas kua Wanatakiwa walipe Sala zao.

Hivyo Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* katika Fatwa yake hii anafananisha na kujumuisha Wanawake wa Kiislam wasiokua wake wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua ni sawa na Wake zake kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuwahi Kuwaamrisha Wanawake waliotoharika kutokana Na Nifasi kua wanatakiwa Walipe, na hivyo hii inamaanisha kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* amewasamehe na kuliondoa Jukumu la Kumuabudu yeye pale Wanawake hao wanapokua kwenye Nifasi kama vile ilivyokua kwenye Hedhi.

Na akasema Imam Al Nawawi kua: **'Wakati Mja mzito anapoona Damu ambayo ina sifa za kama Damu ya Hedhi katika kipindi ambacho ni cha kwake yeye Mwanamke huyyo kua kwenye hedhi, basi kuna mtizamo miwili juu yake jambo hili. Ambapo kwanza ni kulingana na Mtizamo wa Mtizamo wa Imam Al Mawardi muandishi wa Al Hawi, Al Mutawwali, Al Baghawi na wengineo basi wo wamesema kua hii hua ni Damu ya Hedhi. Na hiyo hii hua ni kulingana na Mtizamo wa Kauli Mpya ya Madhhab ya Imam Al Shafii.'**

'Na hii ni kwa sababu Damu Hio hua na sifa na Damu ya Hedhi, kwani hua inatoka katika wakati wa Hedhi na pia hua kuna uwezekano mwengine wa kua Damu hio ikawa ni Damu ya Hedhi au ya Isiadha ila kikanuni basi hua ni Damu ya Hedhi.'*(AlMajmuu)*

Na anasema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi anasema kua: **'Kulingana na Hadi*th ya Ibn Umar Radhi Allahu Anhu* kua almuacha mke wake wakati akiwa katika Hedhi na Umar *Radhi Allahu Anhu* akamuelezea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Talaka hio ambapo nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Mwambie akae nae na asimuache hadi atakapokua Tohara au atakapokua na Uja Uzito' Hivyo katika Hadith hii basi inaonesha kua Uja uzito na Tohara unamaanisha kua Mwanamkehana Hedhi na Mwanamke anapopata Uja uzito hua hapati Hedhi na hivyo Damu anayoiona katika wakati wa Uja Uzito, hua si Hedhi na Imam AhmadIbn Hanbal alisema kua: 'Mwanamke anaweza kujua kua ni Mja mzito kutokana na kua nimwenye kukosa Hedhi yake'***(Al Mughni)***

Nakwa upande mwengine basi kuna baadhi ya wakati hua hazaliwi Mtoto mmoja bali hua zaidi ya Mmoja, yaani kwa mfano kama Mapacha hivyo jee Hukmu yake kuhusiana na Nifasi ikoje?

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Mapacha hua ni Watoto wawili katika Mimba Moja, hivyo kama ikiwa katika Kutoka kwao basi Mtoto wa Kwanza ametofautiana na Mtoto wa pili kwa Mda wa miezi 6, basi Wanazuoni wanakubaliana juu yake kua Hapa kutakua na Vipindi viwili vya Nifasi'***(Al Majmuu)*

Hivyo hio ni kama Watoto watakua wamepishana kwa Miezi 6, lakini kama ikiwa Watoto wamepishana lakini chini ya Miezi 6 yaani tuseme labda baada ya Nusu Saa, Saa moja, Siku,Wiki n.k. lakini si zaidi ya Miezi 5 na siku kadhaa kabla kufikia Miezi 6.

Basi Wanazuoni wametofautiana juu ya Hukmu yake kuhusiana na Suali la kua Jee Nifas ianze kuhesabiwa baada ya kuzaliwa Mtoto wa Kwanza au wa Pili?

Ambapo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Wanakubaliana kua: '**Nifasi Huanza kuhesabiwa pale Fuko la Uzazi linapotoa Nje kila kitu chake, kwa maana hio basi Damu inayotoka baina ya Kuzaliwa kwa Mapacha hua haijakamilisha Sharti hili hadi pale watakapomalizika kutoka watoto hao.**'

Hivyo Wanazuoni hua hawaihesabu Damu hio baina ya kutoka mtoto wa kwanza na wa pili kua ni Nifasi bali wanaihesabu kua ni Hedhi kama alivyosema Al Imam Al Khatib Al Shirbini kua: '**Damu Baina ya Kuzaliwa kwa Mtoto wa Kwanza na wa Pili hua ni Damu ya Hedhi.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Kwa Maana hio basi Fatwa hii hua inamaanisha kua katika hali kama hii basi Nifasi hua inàanza kuhesabiwa baada ya Kuzaliwa Mtoto wa Mwisho.

Ambapo huo ni Mtizamo wa Kwanza lakini Mtizamo wa Pili ni Mtizamo ambao unaenda sambamba na Uthibitisho wa Uchunguzi wa Kisayansi usemao kua: '**Mwanamke Mwenye Mimba hua hapati Hedhi, na hivyo Damu itokayo baina ya Mtoto wa Kwanza na Wa Pili Hua ni Damu ya Nifasi.**'

Ambapo hapa sasa tunarudi kwa Hujjat Ul Islami Mujaddid Ad Din Imam Zukhruf Ad Din Al Shafii Al Thani Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii ambapo yeye amesema katika Fatwa yake kuhusiana na Suali hili kua: **'Nifas huanza kuhesabiwa mara tu baada ya kuzaliwa kwa Mtoto wakwanza baina ya Mapacha.'**

Ambapo huo ndio Mtizamo pia wa Imam Abu Hanifa, Imam Malik, Imam Ahmad Ibn Hanbal na pia ndio Mtizamo wa Mwalimu wake Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Al Ghazali, yaani Imam Abu Maali Al Haramain Al Juwayni.

Na aliulizwa Imam Al Muhaqqiqin Al Aalamah Al Faqih Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: **'Jee ni nini hukmu ya Mwanamke ambae amekua Tohara baada ya siku tatu tu baada ya kujifugua Mtoto wake wa pili, mbali ya kua Mtoto wake wa kwanza alikua Tohara baada ya Siku 40?'**

Imam Al Muhaqqiqin Al Aalamah Al Faqih Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii akajibu kwa kusema kua:**'Mara Tu Mwanamke aliekua katika Hedhi ama Nifasi kutoona Damu yake yaani baada ya kuweka Pamba katika Uke wake ambayo nayo ikatoka ikiwa nyeupe, basi hua anatakiwa kujitiharisha na kufanya Ibada zake ikiwemo Kusali na pia hua inaruhusika kwa Mumewe kuingiliana nae na hii hua bila ya kuangalia kama Damu hio ilikata kutoka kabla ya Siku 40 za Nifasi ama la.'**

‘Na kama Nifas ikiwa itaendelea kutoka baada ya si chini ya siku 15 baada ya kukatika kwake, basi Damu hio itahesabika kua ni Damu ya Hedhi au ya Nifas. Ila kama Nifas itaendelea kutoka baada ya siku 15 baada ya kukatika kwake basi hio itakua ni Damu ya Nifasi na siku hizo 15 itakua ni siku za Kitohara na hivyo atatakiwa kulipa Sal azote alizokua hakuzisali ndani yake.’

‘Ama kuhusiana na Hedhi, basi kama Damu itaendelea kutoka baada ya siku 15 tangu kusita kwake basi hii itamaanisha kua ni Hedhi mpya na kusita kwake hua ndio Tohara yake, hivyo Sala ambazo hazikusaliwa ndaniya siku 15 hizo itabidi zilipwe. Na kama Damu itaendelea kutoa si chini ya siku 15 baada ya kukoma kwake, basi hio itakua ni Hedhi.’*(Al Fatawa Fiqhiyya Al Kubra)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MANII.

❖❖❖❖

Kimaumbile kwa Kila Ibn Adam hua ni mwenye kutokwa na Maji maji ya aina 4 katika sehemu za Siri za Mbeleni. Ambapo aina ya kwanza hua ni Mkojo, aina ya pili hua ni Manii aina ya Tatu hua ni Madhii na aina ya Nne hua ni Wadii.

Ambapo amesema Imam Al-Azhari kua: ‘**Amesema Al Umawi kua Maneno Al-Wadiyy, Madhiyy, na Maniyy hua yanatamkwa kwa kujaziwa uzito wa shaddah mwishoni mwake, ambapo wengine hua wanayatamka bila ya uzito wa shaddah’**

Na bila ya shaka kila Mtu ni mwenye kujua kuhusiana na Mkojo ambayo hua ni Haja ndogo yenye Maumbile ya Maji Maji yenye mchanganyiko wa Uchafu unaojumuisha Maji, Chumvi, Elektrolites (Chemikali zenye kubeba Nguvu ya Nishati) na Yurea. Mchanganyiko huu hupatikana baada ya kuchujwa na Mfumo wa Uchujaji wa Mafigo na Damu na hivyo kutotakikana ndani ya Mwili.Kwani ukibakia ndani yake basi utasababisha Madhara makubwa sana kiafya na ndio Maana Uchafu huanza kutolewa tangu Kuzaliwa kwetu hadi Mwisho wa Maisha yetu, kwa kila siku Mara Kadhaa.

Hivyo mbali ya mkojo ambao huhitajika kutolewa ndani ya Mwili mara kadhaa kwa kila siku, kwa maisha yetu yote lakini pia kuna aina tatu za Maji Maji ambazo huanza kuzalishwa na Kutoka nje ya Miili yetu katika wakati wa baadae wa Maisha yetu yaani pale tunapoanza Kubalegh na hivyo Miili yetu kuanza kututhibitishia kua sasa hivi umeshakua Mtu mzima na una darja ya kua ni *Mukallaf* yaani Mtu mwenye Kutakiwa Kubeba na kutekeleza Majukumu ya Dini Mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae ni Muumba wetu na pia Kutakiwa kutekeleza Majukumu yetu Mbele ya Viumbe wenzetu kwa ujumla.Na hapa sasa ndio unaaza kuandikiwa Dhambi kwa Makosa uliyoyafanya na Kutotekeleza Majukumu yako Mbele ya Mola wako.

Hivyo miongoni mwa Dalili za Kubalegh na hivyo mtu husika kuingia katika darja ya kua ni Mukallaf ni Kutokwa na Manii, ambapo amesema *Allah Subhanah wa Ta’ala* kua:

﴿وَإِذَا بَلَغَ ٱلۡأَطۡفَالُ مِنكُمُ ٱلۡحُلُمَ فَلۡيَسۡتَـٔۡذِنُواْ كَمَا ٱسۡتَـٔۡذَنَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمۡ ءَايَٰتِهِۦ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ﴾

Wa-idha balagha al-atfalu minkumu alhuluma falyasta/dhinoo kama ista/dhana alladheena min qablihim kadhalika yubayyinu Allahu lakum ayatihi waAllahu AAaleemun hakeemun*(Surat Nur 24:59)*

Tafsir: ***Na wanapobaleghe Watoto miongoni mwenu basi na waombe ruhusa kama kama vile walivyokua wakiomba ruhusa waliotangulia kabla yao kiumri. Hivyo ndivyo Allah anavyoweka wazi Aya zake, kwa hakika Allah ni mwingi wa Ilm na ni mwingi wa Hikma.***

Na amesema Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua:

حفظتُ عن رسول الله – صلى الله عليه وسلم –: لا يُتْمَ بعد احتلام، ولا صُمَاتَ يومٍ إلى الليل

Nimehifadhi mimi alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Hakuna Uyatima baada ya kuanza kujimwaga Manii na wala hakuna kukaa kimya tangu Asubuhi hadi usiku'*(Sunnan Abu Daud, Sunnan Al Kubra Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo Neno *Yatima* linatokana na neno *Yatama* ambalo hua linamanisha Kua Yatima, Kua bila ya Baba katika wakati ambao mtu hajafikia umri wa miaka 15, Kua bila ya Mama kwa Mnyama, na kwa upande wa Mwanamke hua ni Yatima pale anapokua hana Mume kutokana na kua hajafikia Umri wa Kuolewa au Mjane wa kufiwa na Mumewe au wa Kuachwa, Kua peke yake, Kufifia, na pia humaanisha kua Mchovu.

Ambapo Imam Raghib Isfahani basi yeye anasema kua: '**Yatima hua ni Kitu au Mtu ambae yuko peke yake, alietengwa na hana mtu yeyote. Kwa mfano *Durra Al Yatima* hua linamaanisha Lulu kubwa sana iliyoghali na isiyokua na mpinzani kwa thamani. Na hivyo neno *Yatima* hua linamaanisha pia Kitu chenye thamani kubwa zaidi ukilinganisha na vyenzake, Mtu aliewapita wenzake katika mambo mbalimbali, Mtoto asiekua na Baba hua anaitwa *Yatima* na Mtoto asiekua na Mama hua anaitwa *Munqati* (yaani Mtu aliekatiwa Mama yake)**'

Hivyo basi mtu anapo balegehe huya si Yatima tena na kukaa kimya tangu asubuhi hadi Jioni kunamaanisha dasturi na mila za kijahili ambapo Mtu alikua anaamua kukaa ndani mwake tangu asubuhi hadi usiku bila ya kusema kitu chochote. Hivyo jambo hili limekatazwa kwani bora kwa mtu kua ni mwenye kufanya dhikr Allah peke yake kuliko kukaa kimya peke yake bila kusema kitu chochote.

Na amesema Imam Tawus kua: '**Mwenye kuzungumza kwa sababu ya kumugopa *Allah Subhanah wa Ta'ala* huya ni bora kuliko yule mwenye kukaa kimya kwa sababu ya kumuogopa *Allah Subhanah wa Ta'ala.'****(Sharh Sunnah Imam Al Baghawi)*

Na amesema *Aisha RadhI Allahu Anha* kua:'**Amesema *Rasul Allah Salallahuy Alayhi wa Salam* kua:**

(رُفِع القلم عن ثلاثةٍ: عن النائم حتى يستيقظَ، وعن الصغير حتى يَكبَرَ، وعن المجنون حتى يعقل، أو يُفِيق)

'Kalamu Imenyenyuliwa kwa watu wa aina tatu, Alielala hadi atakapoamka, Mtoto hadi atakapo Baleghe na Mwendawazimu hadi atakapopona.'*(Sunan Ibn Majah, Sunnan Abu Daud, Suynynan Al Nasai)*

Na amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:

(عرضني رسول الله – صلى الله عليه وسلم – يوم أُحُد في القتال، وأنا ابن أربع عشرة سنةً، فلم يُجِزْني، وعرضني يوم الخندق، وأنا ابن خمس عشرة سنةً، فأجازني.)

Nilijitolea mimi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya kupigana katika siku ya vita vya Uhud, wakati nikiwa na umri wa miaka 14 lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akanikatalia. Na hivyo nikajitolea tena katika Vita vya Khandaq nilipokua na umri wa miaka 15 ambapo nae akanikubalia.

قال نافع: فقدمت على عمر بن عبدالعزيز وهو يومئذٍ خليفة، فحدثته هذا الحديث، فقال: (إن هذا لحد بين الصغير والكبير، فكتب إلى عمَّاله أن يفرضوا لمن كان ابن خمس عشرة سنةً، ومَن كان دون ذلك فاجعلوه في العيال)

Na amesema Nafii kua nilienda mimi kwa Umar Ibn Abd Al Aziz ambae ndie aliekua Khalfia katika wakati wake, na kumnukulia mimi hadithi hii, ambapo nae akasema: 'Huo Ndio Mpaka baina ya Watoto na Watu wazima' hivyo akawaandikia Magavana wake kuhusiana na hali ya waliotimia miaka 15 kuwawekea chini ya sheria, na kuwabakisha wale wenye chini ya umri huo kua ni wenyekua chini ya uangalizi wa wazee wao.*(Sahih Muslim)***

Miongoni mwa Dalili za Kubalegh pia hua ni *Inbiai* yaani kuota Nywele katika sehemu za Siri kama vile alivyosema Imam Is-haq Ibn Rahawayh na Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: **'Kubalegh hua kuna Daraja tatu, Kufikia umri wa miaka 15 au Zaidi na kuota Nywele kwenye sehemu za Siri.'**

Kama ilivyoelezewa katika hadith zifuatazo:

يدل عليه أن النبي – صلى الله عليه وسلم – لما حكَّم سعد بن معاذ في بني قريظة قال: فإني أحكم فيهم أن تقتل مقاتلتهم، وتُسبَى ذراريهم، فقال رسول الله – صلى الله عليه وسلم –: حكمتَ بحُكمِ الملك

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimchagua Sad Ib Muadh*Radhi Allahu Anhu* kua mpatanishaji wa watu wa Banu Quraydha, ambapo naeSad Ib Muadh *Radhi Allahu Anhu*akasema kua: 'Nimehukumu mimi kua Wapiganaji wao wauliwe na watoto wao wafanywe kua Mateka'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Umetoa Hukumu kulingana na Hukmu za Kifalme'(Musnad Imam Ahmad, Musnad At Tayalisi)***

Na anasema Atiyah Al Quraydha *Radhi Allahu Anhu* kua:

(كنتُ غلامًا يومَ حكم سعد بن معاذ – رضي الله عنه – في بني قُرَيظة أن يقتلَ مقاتلتهم وتسبى ذراريهم، فشكُّوا فيَّ، فلم يجدوني أنبتُّ الشعر، فها أنا ذا بين أظهركم)

Mimi nilikua mtoto mdogo katika siku ambayo Sad Ibn Muadh alipotoa Hukumu juu ya Banu Quraydha kua Wapiganaji wao Wauliwe na Watoto wao wafanywe kua Mateka, hivyo wakawa na Shaka juu yangu wakanitazama na wakanikuta kua sijaota Nywele bado, na sasa hivi mimi hapa niko pamoja nanyi.

Ambapo kwa upande wa Mwanammke basi hua ni kupata siku za Hedhi kwani amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* kua:**

لا يقبلُ الله صلاةَ حائضٍ إلا بخمار

'Allah hazikubali Sala za Mwenye kupata Hedhi isipokua atakapokua amevaa khimar.'*(Sunan Abu Daud)*

Yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* hazikubali Sala za Mwanamke alie baleghe hadi pale Mwanammke huyo atakapokua amejihifadhi kimavazi katika wakati wa Ibada ya Sala yake hio.

Ambapo kwa upande wa Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* aliulizwa kuhusiana na umri wa mtu kuitw Yatima ambapo nae akasema:

كتبت إلي تسألني متى ينقضي يتم اليتيم، والله إن الرجل ليُنبت لحيته، ولكنه ضعيف في نفسه ضعيف في بذلها، فإذا أخذ لنفسه من خيرات الناس زال يتمه.

Mnaniandikia Barua kuulizia kuhusiana na mwisho wa Uyatima, Wa Allahi Mwanamme anaweza akawa ameshaota Ndevu lakini akawa ni dhaifu wa kujisimamia yeye mwenye Nafis yake na katika kutoa katika Mali yake, hivyo kama Mtu akiweza kujisimamia kwa Mema wafanyayo watu basi Uyatima wake hutoweka. *(Sahih Muslim)*

Hiyo kulingana na vithibitisho hivi basi tunaona kua kuna tofauti baina ya Umri wa Kubaleghe na Umri wa Kukua Kiakili, ambapo Umri wa Kukua kiakili kama alivyoelzea Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambao ndio hua Umri wa kubebeshwa Majukumu na hivyo Mhusika huya si mwenye kuhesabika kua ni Yatima na hivyo anaweza kupewa Mali yake akasimamia, au akapewa msaada wa Zakkah, n.k

Kama alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَٱبْتَلُواْ ٱلْيَتَامَىٰ حَتَّىٰٓ إِذَا بَلَغُواْ النِّكَاحَ فَإِنْ آنَسْتُمْ مِّنْهُمْ رُشْداً فَٱدْفَعُواْ إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ وَلاَ تَأْكُلُوهَآ إِسْرَافاً وَبِدَاراً أَن يَكْبَرُواْ وَمَن كَانَ غَنِيّاً فَلْيَسْتَعْفِفْ وَمَن كَانَ فَقِيراً فَلْيَأْكُلْ بِٱلْمَعْرُوفِ فَإِذَا دَفَعْتُمْ إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ فَأَشْهِدُواْ عَلَيْهِمْ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ حَسِيباً﴾

Waibtaloo alyatamahatta idha balaghoo alnnikaha fa-in anastum minhum rushdan faidfaAAoo ilayhim amwalahum wala ta/kulooha israfan wabidharan an yakbaroo waman kana ghaniyyan falyastaAAfif waman kana faqeeran falya/kul bialmaAAroofi fa-idha dafaAAtum ilayhim amwalahum faashhidoo AAalayhim wakafa biAllahi haseeban.*(Surat An Nisaa 4:06)*

Tafsir: ***Na wajaribuni (Kiakili na ufaham wao) Mayatima hadi wawe wamebaleghe na kufikia umri wa kuoa, na mkiwaona wana ufaham mzuri, basi wapeni mali zao, na wala msizitumie kwa Israfu kutokana na kua na khofu kua watakua wakubwa. Na kama ikiwa mmoja miongoni mwenu ni Tajiri basi asichukue malipo. lakini kama akiwa Fukara basi na wacha na achukue kinachostahiki, na kisha mtakapowakabidhi Mali zao basi kuwe na shahidi juu yao na kwa hakika anatosheleza Allah Kuchukua Mahesabu.***

Ambapo aya imetumia neno *Bala* ambalo linamaanisha Kujaribu, Kufanyia Mtihani iwe kwa ajili ya Kupandisha Darja au kwa Kuadhirisha, Kuthibitisha, Kusimama. Kufadhili,

Hivyo aya inatubainishia kua kwa kila mwenye kulea Yatima basi baada ya kufika mda wa kumalizika kipindi cha kulelewa Mayatima yaani wamesha baleghe basi wanatakiwa kujaribiwa ufaham wao kuangaliwa kama wanao uwezo wa kusimamia Mali zao, ambapo kwa upande wa Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi mtizamo wao kuhusiana na Umri stahiki kwa mtoto kua tayari ameshakua mkubwa hua ni miaka 17 wa Mwanamke na miaka 18 wa Mwanamme.

Na kubaleghe pia ndio unapoanza kulipwa Thawabu Kumi kwa kila Jema Moja utakalokifanya. Ambapo Maovu hayo na Mema yako ndio yatakayokuja Kuhesabiwa mbele ya Mola wako katika Siku ya Malipo na hivyo kuonesha Kama Ulikua na Shukran mbele ya Mola wako au Ulikua huna Shukran mbele yake na utalipwa ipasavyo bila Kudhulumiwa kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua**:**

﴿مَن جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۖ وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ﴾

Man jaa bilhasanati falahu AAashru amthaliha waman jaa bissayyi-ati fala yujza illa mithlaha wahum la yudhlamoon.*(Surat Al Anaam 6:160)*

*Tafsir:****Atakaekuja (Katika Siku ya Malipo) Akiwa na MemaBasi Atalipwa Mara Kumi Mithili yakeNa Atakaekuja Na Maovu (Katika Siku ya Malipo)Basi Hatolipwa isipokua Mithili yakeNa Wala hawatodhulumiwa.***

Ambapo mbali ya kua baadhi ya Wanazuoni wametafsiri kua Hasanat katika aya hii hua inamaanisha Kalimat Tawhid yaani *La Ilaha Illa Allah* iliyotamkwa kwa Ikhlasi na Sayyiati inamaanisha Shirk kama alivyosema Imam Ibn Jarir At Tabari.

Lakini pia kuna Hadith isemayo kua: **‘Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua kwa Kila atakaefunga Siku tatu ndani ya Kila mwezi basi hua ni sawa aliefunga Mwaka mzima kwani**

Kila atakaekuja na Jema moja katika Siku ya Malipo basi atalipwa Mara 10 yake na kila atakaekuja na Ovu moja basi hatolipwa isipokua Fidia ya Ovu hilo hilo.' *(Imam At Tirmidhii)*

Ambapo kuna Hadith Al Quds pia isemayo kua:

إِنَّ اللَّهَ كَتَبَ الحَسَناتِ والسَّيِّئاتِ ثُمَّ بَيَّنَ ذلكَ، فمَن هَمَّ بحَسَنَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْها، كَتَبَها اللَّهُ له عِنْدَهُ حَسَنَةً كامِلَةً، فإنْ هو هَمَّ بها فَعَمِلَها، كَتَبَها اللَّهُ له عِنْدَهُ عَشْرَ حَسَناتٍ، إلى سَبْعِ مِائَةِ ضِعْفٍ، إلى أضْعافٍ كَثِيرَةٍ، ومَن هَمَّ بسَيِّئَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْها، كَتَبَها اللَّهُ له عِنْدَهُ حَسَنَةً كامِلَةً، فإنْ هو هَمَّ بها فَعَمِلَها، كَتَبَها اللَّهُ له سَيِّئَةً واحِدَةً.

'Hakika ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameandika Mema na maovu na kisha baina yake basi yeyote alienuia kufanya Jema na ikawa hakuweza kulifanya basi ataandikiwa kua amefanya Jema hilo kwa Malipo ya mara moja. Na kama akifanikiwa kulifanya basi ataandikiwa kua amelifanya Jema hilo kwa Malipo ya mara 10 mithili yake.

Na atakaenuia kufanya Ovu na ikawa hakulifanya basi ataandikiwa kua amefanya Jema moja. Na kama akilifanya Ovu hilo basi ataandikiwa kua amefanya Ovu Moja, labda pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* aamue kulifuta Hivyo hakuna atakaeangamizwa na A*llah Sabhanah wa Ta'ala* isipokua yule atakaejiangamiza Nafsi yake mwenyewe. *(Sahih Bukhari, Sahih Muslim na Sunnan An Nasai)*

Na amesema *Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu* kua amsema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua:

مَن هَمَّ بحَسَنَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْها، كُتِبَتْ له حَسَنَةً، ومَن هَمَّ بحَسَنَةٍ فَعَمِلَها، كُتِبَتْ له عَشْرًا إلى سَبْعِ مِئَةِ ضِعْفٍ، ومَن هَمَّ بسَيِّئَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْها، لَمْ تُكْتَبْ، وإنْ عَمِلَها كُتِبَتْ.

'Yeyote alienuia kufanya Jema na ikawa hakuweza kulifanya basi ataandikiwa kua amefanya Jema hilo kwa Malipo ya mara moja. Na kama akifanikiwa kulifanya basi ataandikiwa kua amelifanya Jema hilo kwa Malipo ya mara 10 hadi mara 700 mithili yake.

Na atakaenuia kufanya Ovu na ikawa hakulifanya basi hatoandikiwa kitu. Na kama akilifanya Ovu hilo basi ataandikiwa kua amefanya Ovu Moja.'*(Sahih Muslim)*

Na akasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Qur'ani kua;

﴿مَّثَلُ ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمۡوَٰلَهُمۡ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَنۢبَتَتۡ سَبۡعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُنۢبُلَةٖ مِّاْئَةُ حَبَّةٖۗ وَٱللَّهُ يُضَٰعِفُ لِمَن يَشَآءُۚ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ﴾

Mathalu alladheena yunfiqoona amwalahum fee sabeeli Allahi kamathali habbatin anbatat sabAAa sanabila fee kulli sunbulatin mi-atu habbatin waAllahu yudhaAAifu liman yashao waAllahu wasiAAun AAaleemun*(Surat Al Baqarah 2:261)*

Tafsir: ***Mithili ya wale wanaotumia Mali zao kwa ajili ya Allah Subhanah wa Ta'ala hua ni mithili ya Punje ya Ngano ambayo huota na kutoa Mashuke 7, ambap kila shuke moja hutoa Punje Mia, na Allah Subhanah wa Ta'ala huzidishia kwa yule amtakae na Allah ni mwenye kukizunguka kila kitu na ni mwenye kujua juu ya kila kitu.***

Hivyo Aya na hadith zinatuonesha wingi wa Rehma na Ukarimu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kuwapendelea Waja wake waliofikia Umri wa Mukallaf na kisha wakawa ni wenye kufanya Mema, na pia namna anavyowachukulia kutokana na kasoro zinazotokana na Udhaifu wao Kimaumbile kwani kama si hivyo basi isingwezekana kwa Ibn Adam kupata mafanikio kutokana na Mema yao kwa sababu Maovu hua ni daima yenye kuwazidi Ibn Adam kutokana na Matamano ya Nafsi na pia vishawishi vya Adui yao yaani Ibilisi.

Na miongoni mwa mambo yanayosabisha maovu kwa Ibn Adam wengi sana ni kutoweza kudhbiti sehemu zao za Siri ambazo kimaumbile kwa Kila Ibn Adam hua ni mwenye kutokwa na Maji maji ya aina 4 katika sehemu za Siri za Mbeleni.Ambapo aina ya kwanza hua ni Mkojo, aina ya pili hua ni Manii aina ya Tatu hua ni Madhii na aina ya Nne hua ni Wadii. Na tukiachana na Mkojo basi aina zilizobakia huonekana baada ya Mtu kubaleghe. Iwe Mtu huyo ni Mwanamme au Mwanamke. Na hivyo kabla ya kuendelea basi na tufafanue maana ya Manii, Madhii na Wadi.

Ambapo Wanazuoni wanakubaliana kua Kumwagwa kwa Manii iwe katika wakati wa kulala usingizini, kwenye Ndoto, nje ya usingizi au kwa makusudi kwamfano kwa kujipapasa ama kujichua ni Dalili zinazoonesha kua Mtu huysika ameshabaleghe kama ilivyosema kwenye Mawsuah Fiqhiyyah Al Kuwaitiyyah kua: **'Kumwagwa kwa Manii na Mwanamme au Mwanamke wakati akiwa amelala au yuko macho basi humaanisha kuwadia kwa wakati wa kubaleghe'**

Ambapo anasema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua: **'Ama kuhusiana na kumwagwa kwa Manii, basi Manii yanapotoka ambayo hua ni meupe, huya ni yeny enguvu ya mchupo ambayo kutokana nayo ndio huumbwa Mtoto katika wakati wa kuingiliana, au kumwagwa katika wakati ambao Mtu amelala, au akiwa macho basi hizi zote huya ni dalii za kubaleghe kwa mhusika'**

Ambapo amesema Imam An Nawawi kua: '**Kumwagwa kwa Manii hua ni dalili ya kubaleghe kwa mhuysika na huanzia mtu anapotimia umri wa miaka tisa.'** *(Minhaj al-Tolibin wa Umdah Al Muftin)*

Hivyo basi kuhusiana na Manii basi hua ni Maji yenye Rangi ya weupe wa Maziwa na Mazito ambayo hutoka katika Viungo vya Uzazi kwa hali ya Nguvu ya Mchupo, utokanao na hali ya Kufanikisha kusudio linalotokana na Matamanio ya Kimwili ambalo humpelekea mwenye Kufanikisha kusudio hilo kua ni mwenye Kuridhika kutokana na Raha iliyojaa Msisimko baada ya Kupatikana kwa fanikio hilo.

Ambapo Hukmu ya Manii mbali ya kua si Najis kama tutakavyofafanua hapo baadae lakini yanapotoka ndani ya Mwili basi humpelekea Mhusika alietokwa nayo kua ni mwenye Wajibu wa kujitoharisha kwa kukoga Janaba. Iwe kutoka huko kumetokana na wakati Mtu husika akiwa Usingizini au yumacho.

Madhii hua ni Maji ambayo yanatoka kabla ya Kutoka Manii, maji haya hua ni mepesi na hutoka pale Mtu anapokua na Hamu ya Kuingiliana Kimwili na Mwenza wake.Madhii yanapotoka hua ni yenye jukumu la kuitayarisha na kuisafisha Njia ya Mkojo Ili Manii ambayo hua yanabeba mbegu za Uzazi yawe na urahisi wa kufanikisha Malengo ya Kumpatia hisia ya Raha na Utulivu anaeyatoa na pia lengo la kufanikisha kuendeleza Kizazi ambayo ndio Malengo Makuu pia ya Ndoa.

Na kutokana na Wepesi na Ulaini wake basi Madhii yanapomtoka Mtu husika basi hua hawezi kuhisi kihisia ila anaweza kuyaona baada ya kutoka kwake.Na kutoka kwa Madhii hua haukupunguzi nguvu au uwezo wa Matamanio bali hua ni yenye kuongeza muamsho wa Hamu ya Matamanio husika.

Ama kuhusiana na Wadi basi hua ni Maji ambayo mazito kidogo Kuliko Madhii na mepesi kuliko Manii na hua yana rangi ya Njano kwa mbaali.Ambapo kutoka kwake Wadi hua ni kutokana na haja ya kujisaidia Haja ndogo.Na hivyo basi Wadi hua ni Maji yenye kuambatana na Mkojo na hutoka kabla ya kutoka Mkojo au baada yake.

Hivyo Wadi hua ni tofauti na Manii na Madhii kwa sababu ya kua Wadi ni Maji ambayo hayahusiani na hali ya hisia za Hamu ya Matamanio, lakini hutoka kama Madhii, kutokana na kua si yenye kutoka kwa Nguvu kama Manii au Mkojo.

Naam..amesema Mujaddid Ad Din Imam Al Mujtahid, Imam Muhammad Idris Al Shafii kua:

كُلِّ مَا خَرَجَ مِنْ ذَكَرٍ مِنْ رُطُوبَةِ بَوْلٍ، أَوْ مَذْيٍ أَوْ وَدْيٍ أَوْ مَا لَا يُعْرَفُ، أَوْ يُعْرَفُ فَهُوَ نَجِسٌ كُلُّهُ مَا خَلَا الْمَنِي

‘Kila kitu kitakachotoka katika Uume, iwe kitu hicho ni Mkojo, Madhii, Wadii au kitu chochote kinachojulikana au kisichojulikana basi Hukmu yake hua ni kua Kitu hicho ni Najis, Isipokua Manii.’*(Al Umm)*

Ambapo Fatwa hii ni kwa Upande wa Wanawake pia kama tutakavyofafanua hapo baadae In-shaa Allah.

Ambapo neno Manii limetokana na neno ambalo *Mana* kwa kilugha hua linamaanisha Kushawishi Kimatamanio.

Neno *Mana* ndio lililotoa neno *Amna* ambalo humaanisha Kutamani na likatoa neno *Maniytun* ambalo humaanisha Kifo, na likatoa neno *Munyatu*n linalomaanisha Kitu Kinachotamaniwa na likatoa neno *Tamanna* yaani Kutamani au kua na Hamu, na pia Likatoa neno *Tumnuna* linalomaanisha Kutoa.

Ambapo neno Mana pia ndio lililotoa neno Al Istimnaa ambalo humaanisha Kutumia Kitu kwa ajili ya Kujiridhisha kwa Matamanio ya kutoa Manii bila ya njia ya kuingiliana kimwili, ambapo anasema Imam Al Shafii kua:

فَلَا يَحِلُّ الْعَمَلُ بِالذَّكَرِ إِلَّا فِي الزَّوْجَةِ أَوْ فِي مِلْكِ الْيَمِينِ وَلَا يَحِلُّ الِاسْتِمْنَاءُ

Hairuhusiki Kuutumia Uume isipokua kutokana na Mke wake Mtu husika au Mtumwa wake Na Istimnaa hua haikubaliki.*(Al Umm)*

Na imesemwa kwenye *Mawsuah Al Fiqhiyyah Al Kuwaitiya* kua: '**Neno Al Istimnaa au Kujichua ni neno lililtokana na neno Istimani yaani Kutumia jitihada kwa ajili ya kumwaga Manii, ambapo neno hili hua linamaanisha Kumwaga Manii bila ya kutumia njia ya Kuingiliana kimwili, ambayo hua ni njia ya kutumia mkono isiyoruhusika kwa ajili ya kufanikisha matamanio ya kimwili au kwa njia iliyoruhusiwa kwa kutumianjia ya mkono wa mke wake Mtu husika.'** *(Al-Mausu'ah al-Fiqhiyyah al-Kuwaitiyyah*)

Na bila ya shaka neno *Mana* ndio lililotoa neno *Maniyyun* ambalo humaanisha Manii, Tone la Kitu kinachomwagwa Tone la Manii na pia humaanisha Viini Hai vya Uhai vilivyomo ndani ya Manii.

Kama anavyoelezea kuhusiana nayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Njia ya kuhoji pale aliposema:

﴿أَيَحْسَبُ ٱلْإِنسَانُ أَن يُتْرَكَ سُدًى ۞ أَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِّن مَّنِيٍّ يُمْنَىٰ﴾

Ayahsabu al-insanu an yutraka sudan; Alam yaku nutfatan min manayyin yumna*(Surat Al Qiyama 75:36-37)*

*Tafsir:**Hivi Anajihesabu Mtu kua ataachiwa tu hivi hivi bila ya Kuadhibiwa au Kulipwa kutokana na Maamrisho aliyoamrishwa na Mola wake? Hivi Jee Hakua Katika Hali ya kuani Tone la Manii lililomwagwa?***

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakallimin Imam Al Mushaqqiqin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kuhusiana na aya hizi kua:**'*Allah Subhanah wa Ta'ala* anahoji kua Hivi Watu wanafikiria kua Wameumbwa tu kwa ajili ya Mchezo na hawatoulizwa kitu baada ya kufa kwao na kufufuliwa katika Siku ya Malipo?'**

'Kwani Kama Watu wanafikiria hivyo basi inamaanisha kua Wanafikiria pia kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* hajui chochoteJuu ya kila wakifanyacho Hapa Ulimwenguni, jambo ambalo haliingii akilini kabisa.'

Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* anathibitisha kua kila Ibn Adam hapa Ulimwenguni ameumbwa kutokana Tone la Manii lililomwagwa, na hivyo kumaanisha kua Kitendo hicho cha kumwagwa huko kwa Viini hai vya Ibn Adam sio Jambo kubwa Sana na lisilotilika maanani.' *(Mafatih Al Ghayb)*

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaendelea kutuelezea kuhusiana na Kutotilika maanani kwa kitu hicho Kwa kusema kua:

﴿أَلَمْ نَخْلُقكُّم مِّن مَّآءٍ مَّهِينٍ﴾

Alam nakhluqkum min ma-in maheenin*(Surat Al Mursalat 77:20)*

*Tafsir: **hivi Hatujakuumbeni Nyinyi kutokana na Maji Machache yasiyokua na Thamani?***

Na kisha akasema tena kwa kuthibitisha kua:

﴿فَلْيَنظُرِ ٱلْإِنسَانُ مِمَّ خُلِقَ ۞ خُلِقَ مِن مَّآءٍ دَافِقٍ﴾

Falyan<u>dh</u>uri al-ins<u>a</u>nu mimma khuliqa; Khuliqa min m<u>a</u>-in d<u>a</u>fiqin*(Surat Tariq 86:5-6)*

*Tafsir:**Hebu Na Ajiangalie Mtu Ameumbwa Kutokana na nini? Ameumbwa Kutokana na Maji yatokayo kwa kasi ya Mchupo.***

Naam..hivyo aya hizi ni zenye kuelezea Asili ya Kila Ibn Adam Ulimwenguni kua ni Kutokana na Kitu kidogo sana, Kisichokua na Thamani, ambacho Hutoka Ndani ya Mwili kwa njia ya Mchupo.

Lakini hapo hapo kitu kidogo hicho kisichokua na Thamani kiasi ya kua kikikumwagikia basi huwezi kubakia nacho bali lazima utatafuta njia ya Kukifuta, kutokana na kuonekana kua ni ukinyaa wake basi ndicho kitu ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* amemtoa kila Ibn Adam ndani yake, kutokana na Sifa yake ya Jina Tukufu la *Al Khaliqu ladhii Khalaqa Fasawwa* - Muumbaji ambae ameumba Kila kitu na Kisha Kukiweka Sawia kila hicho alichokiumba kutokana na kua yeye ndie *Rabb Al Alamiin* - Mola Mlezi na Msimamzi wa Ulimwengu wote na Viumbe vyote vilivyomo ndani yake tangu mwanzo wake Ulimwengu huyo na vitu vyake vyote vilivyomo ndani yake tangu mwanzo wake hadi mwisho wake. Kama zinavyosema Aya baada ya *Bismi Allahi Rahmani Rahiim:*

﴿بِسْمِ اللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۞ سَبِّحِ ٱسْمَ رَبِّكَ ٱلأَعْلَىٰ ۞ ٱلَّذِى خَلَقَ فَسَوَّىٰ ۞ وَٱلَّذِى قَدَّرَ فَهَدَىٰ﴾

Sabbi<u>h</u>i isma rabbika al-aAAl<u>a;</u> Alla<u>dh</u>ee khalaqa fasaww<u>a;</u> Waalla<u>dh</u>ee qaddara fahad<u>a</u> *(Surat Al Aala 87:1-3)*

*Tafsir :**Litukuze Jina la Mola Wako Mtukufu, alieumba kila kitu na kukiweka sawia na alie kikadiria kila kitu na kukiongoza.***

Ambapo anasema Jarrah Allah Imam Abu Qasim Al Zamakhshari kuhusiana na maneno ya Aya hizi kua: 'Aya zinatuonesha uongofu wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya kila kitu kilicho kizuri na kilicho kibaya kwa Viumbe wake, iwe kuhusiana na Vyakula, Dawa na kila kinachohitajiwa na Viumbe wake wakiwemo Wanyama, Ndege, Wadudu n.k Aya hizi hakuna mwenye uwezo wa Kuzielezea ipasavyo hivyo *Subhanah Rabbi Al Aala!'*

Na mingoni mwa vilivyoumbwa nae *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi kama tunavyoona kua ni haya Maji Yasiyotilika Maanani yatokayo kwa mchupo yaani Manii ambayo ndio chanzo cha Kila Ibn Adam basi ni Tohara kama alivyosema Imam Muhammad Idris Al Shafii. Lakini hata hivyo basi yakitoka Humbidi Mtu husika aende akajtoharishe kwa kukoga Janaba.

Kwani Amesema Abu Kurayb kua amesema Yunus Ibn Bakir kua amesema Abd Al Hamid Ibn Bahram kua amesema Shahr Ibn Hawshab kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

حضَرَتْ عِصابةٌ مِنَ اليَهودِ نَبيَّ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ يَومًا، فقالوا: يا أبا القاسِمِ، حَدِّثْنا عن – خِلالٍ نَسألُكَ عنهُنَّ، لا يَعلَمُهنَّ إلَّا نَبيٌّ. قال: سَلوني عمَّا شِئتُم، ولكنِ اجعَلوا لي ذِمَّةَ اللهِ وما أخَذَ يَعقوبُ عليه السَّلامُ على بَنيهِ: لَئِن حَدَّثتُكم شَيئًا فعَرَفتُموهُ، لَتُتابِعُنِّي على الإسلامِ. قالوا: فذلك لكَ.

قال: فسَلوني عمَّا شِئتُم. قالوا: أخبِرْنا عن أربَعِ خِلالٍ نَسألُكَ عنهُنَّ؛ أخبِرْنا أيَّ الطَّعامِ حرَّمَ إسرائيلُ على نَفْسِه مِن قَبلِ أنْ تُنزَّلَ التَّوراةُ؟ وأخبِرْنا كيف ماءُ المرأةِ وماءُ الرَّجُلِ، كيف يَكونُ الذَّكَرُ منه؟ وأخبِرْنا كيف هذا النَّبيُّ الأُمِّيُّ في النَّومِ؟ ومَن وَليُّه مِنَ المَلائِكةِ؟ قال: فعليكم عَهدُ اللهِ وميثاقُهُ لَئِن أنا أخبَرتُكم لَتُتابِعُنِّي. قال: فأعطَوْهُ ما شاءَ مِن عَهدٍ وميثاقٍ، قال: فأنشُدُكم بالذي أنزَلَ التَّوراةَ على موسى صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ هل تَعلَمونَ أنَّ إسرائيلَ يَعقوبَ عليه السَّلامُ مَرِضَ مَرَضًا شَديدًا، وطالَ سَقَمُه، فنذَرَ للهِ نَذرًا لَئِن شفاهُ اللهُ تَعالى مِن سَقَمِه لَيُحرِّمَنَّ أحَبَّ الشَّرابِ إليه، وأحَبَّ الطَّعامِ إليه، وكان أحَبُّ الطَّعامِ إليه لُحمانَ الإبِلِ، وأحَبُّ الشَّرابِ إليه ألبانَها؟ قالوا: اللَّهمَّ نَعَمْ. قال: اللَّهمَّ اشهَدْ عليهم، فأنشُدُكم باللهِ الذي لا إلهَ إلَّا هو الذي أنزَلَ التَّوراةَ على موسى، هل تَعلَمونَ أنَّ ماءَ الرَّجُلِ أبيَضُ غَليظٌ، وأنَّ ماءَ المرأةِ أصفَرُ رَقيقٌ، فأيُّهما عَلا كان له الوَلَدُ والشَّبَهُ بإذْنِ اللهِ؛ إنْ علا ماءُ الرَّجُلِ على ماءِ المرأةِ كان ذَكَرًا بإذْنِ اللهِ، وإنْ علا ماءُ المرأةِ على ماءِ الرَّجُلِ كان أُنثى بإذْنِ اللهِ؟ قالوا: اللَّهمَّ نَعَمْ. قال: اللَّهمَّ اشهَدْ عليهم، فأنشُدُكم بالذي أنزَلَ التَّوراةَ على موسى هل تَعلَمونَ أنَّ هذا النَّبيَّ الأُمِّيَّ تَنامُ عَيناهُ ولا يَنامُ قَلبُه؟ قالوا: اللَّهمَّ نَعَمْ. قال: اللَّهمَّ اشهَدْ. قالوا: وأنتَ الآنَ فحَدِّثْنا مَن وَليُّكَ مِن المَلائِكةِ؟ فعِندَها نُجامِعُكَ، أو نُفارِقُكَ. قال: فإنَّ وَلِيِّي جِبريلُ عليه السَّلامُ، ولم يَبعَثِ اللهُ نَبيًّا قَطُّ إلَّا وهو وَليُّه. قالوا: فعِندَها نُفارِقُكَ، لو كان وَليُّكَ سِواهُ مِنَ المَلائِكةِ لَتابَعناكَ وصَدَّقناكَ. قال: فما يَمنَعُكم أنْ تُصَدِّقوهُ؟ قالوا: إنَّه عَدوُّنا. قال: فعِندَ ذلك قال اللهُ عزَّ وجلَّ: {قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ} [البقرة: 97]، إلى قَولِهِ عزَّ وجلَّ: {كِتَابَ اللَّهِ وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ كَأَنَّهُمْ لَا يَعْلَمُونَ} [البقرة: 101]، فعِندَ ذلك باؤوا بغَضَبٍ على غَضَبٍ... الآيةَ

Kuna Kundi la Mayahudi walikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kumwambia kua: 'Ewe Abu Qasim hebu tuambie kuhusiana na Sifa za haya tutakayokuulizia Juu yake, ambayo ni Mtume tu ndie aneweza kuyajua juu yake.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Niulizeni Mnalotaka, lakini nipeni Hifadhi ya Allah na Ahadi ya Makubaliano ambayo Yaqub aliichukua kutoka kwa Watoto wake kwa kuwaambia kua:Kama Nikikuambieni kuhusiana na Kitu ambacho Mtakifahamu basi mtamifuata Mimi katika Uislam.'**

Mayahudi hao wakasema: 'Makubaliano hayo ni haki yako.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* akasema: 'Sawa Niulizeni Mtakacho.'

Mayahudi wakasema: 'Tuambie kuhusiana na Sifa za haya mambo manne tutakayokuuliza ambayo ni yafuatayo:Tuambie Jee ni Chakula Gani ambacho Israil (Nabii Yaqub) alijiharamishia mwenyewe kabla ya kushuka kwa Tawrat? Tuambie Kuhusiana na Manii ya Mwanamme na ya Mwanamke yakoje? Na Mtoto wa Kiume anapatikanaje?'.

Na tuambie kuhusianana ni Vipi Huyu Mtume asiejua kusoma hua analalaje?..

Na ni nani Malaika wake Muongozaji?.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hivyo tunakubaliana kua kuna Makubaliano na Allah juu yenu kua kama nikikuambieni basi Mtanifuata?.'**

Ambapo Mayahudi hao wakakubaliana nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Sawa, hivyo nakuulizeni kwa Jina la yule ambae ndie alieishusha Tawrat kwa Musa. Kua Jee Mnajua kua Israil Yaqub aliumwa sana na Maradhi yake yalikaa kwa mda mrefu hivyo akaweza Nadhiri kwa Allah Subhanah wa Ta'ala, kua kama akimponesha kutokana na Maradhi hayo basi atajiramishia kutokana na Chakula chake akipendacho na Kinywaji akipendacho Na chakula chake akipendacho ni Nyama ya Ngamia na Kinywaji chake akipendacho ni Maziwa ya Ngamia?.'

Mayahudi hao wakasema: 'Naam Wa Allahi ni Sahih.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Ya Allah kua Shahidi Dhidi yao! Nami nakuulizeni nyinyi kwa jina la yule ambae ndie alieiteremsha Tawrat kwa Musa kua: 'Jee mnaju kua Manii ya Mwanamme ni Meupe na mazito na Manii ya Mwanamke ni mepesi na yana rangi ya Njano Hivyo yoyote kati ya yao yatakayokua na nguvu zaidi basi yatatoa Mtoto aliefanana nae.'**

'Wa Allahi Jee kama Manii ya Mwanamme yatakua juu zaidi ya Mwanamke basi Mtoto atakua wa Kiume kwa Idhini ya Allah na kama Manii ya Mwanamke yakiwa juu zaidi basi kwa Idhini ya Allah atakua Mtoto wa Kike?'

Mayahudi wakasema: 'Wa Allahi Naam Sahih'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Ya Allah Kua Shahidi dhidi yao,nami nakuulizeni kwa Jina la yule ambae ndie aliemshushia Musa Tawrat Hivi Jee mnajua kua haya Macho ya Nabii Asiejua Kusoma kua yanalala na lakini Moyo wake haulali?'**

Mayahudi hao wakasema: 'Naam w Allahi hivyo sasa tuambie kuhusiana na Muongozi wako miongoni mwa Malaika? kisha nasi tutajumuika nawe au tutaachana nawe.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema : 'Malaika wangu Muongozi nia Jibril *Alayhi Salam* na Allah hakutuma Mtume isipokua Malaika wake Kiongozj alikua ni Jibril.'**

Mayahudi wakasema: 'Hivyo tutaachana nawe,kwani kama Malaika wako kiongozi angekua mwengine zaidi yake basi sisi tungekufuata na kukuamini.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza: 'Ah! Sasa ni kitu gani kilichokuzuieni kua Msimuamini?.'**

Mayahudi wakasema: 'Kwa Sababu Jibril ni Adui yetu.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Kama ni hivyo basi amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿قُلْ مَن كَانَ عَدُوًّا لِّجِبْرِيلَ فَإِنَّهُۥ نَزَّلَهُۥ عَلَىٰ قَلْبِكَ بِإِذْنِ ٱللَّهِ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَهُدًى وَبُشْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ۞ مَن كَانَ عَدُوًّا لِّلَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَرُسُلِهِۦ وَجِبْرِيلَ وَمِيكَىٰلَ فَإِنَّ ٱللَّهَ عَدُوٌّ لِّلْكَٰفِرِينَ ۞ وَلَقَدْ أَنزَلْنَآ إِلَيْكَ ءَايَٰتٍۭ بَيِّنَٰتٍ ۖ وَمَا يَكْفُرُ بِهَآ إِلَّا ٱلْفَٰسِقُونَ ۞ أَوَكُلَّمَا عَٰهَدُوا۟ عَهْدًا نَّبَذَهُۥ فَرِيقٌ مِّنْهُم ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ۞ وَلَمَّا جَآءَهُمْ رَسُولٌ مِّنْ عِندِ ٱللَّهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ نَبَذَ فَرِيقٌ مِّنَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ كِتَٰبَ ٱللَّهِ وَرَآءَ ظُهُورِهِمْ كَأَنَّهُمْ لَا يَعْلَمُونَ﴾

Qul man kana AAaduwwan lijibreela fa-innahu nazzalahu AAala qalbika bi-idhni Allahi musaddiqan lima bayna yadayhi wahudan wabushra lilmu/mineena; Man kana AAaduwwan lillahi wamala-ikatihi warusulihi wajibreela wameekala fa-inna Allaha AAaduwwun lilkafireena; Walaqad anzalna ilayka ayatin bayyinatin wama yakfuru biha illa alfasiqoona; Awa kullama AAahadoo AAahdan nabadhahu fareequn minhum bal aktharuhum la yu/minoonaWalamma jaahum rasoolun min AAindi Allahi musaddiqun lima maAAahum nabatha fareequn mina alladheena ootoo alkitaba kitaba Allahi waraa *th*uhoorihim kaannahum la yaAAlamoona *(Surat Al Baqara 2:97-101)*

Tafsir: **Sema (Ewe *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam)* kua Yeyote yule atakaekua Adui wa Jibril(basi Mwache afe kwa hasira zakeKwani *(Allah Subhanah wa Ta'ala)* ameishuha Hii(Qur'an) ndani ya Moyo wako. Kwa Idhini ya Allah Kuthibitisha vilivyokuja hapo kabla(Tawrat na Injil)Na Uongofu na Bashirio Jema kwa Waumini. Atakaekua Adui wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mitume wakeJibril na Mikail basi kwa hakika *Allah Subhanah wa Ta'ala* ni Adui kwa Makafiri. Na kwa hakika sisi tumetuma kwako wewe Aya zizlizowazi na hakuna atakaezikaa isispokua ni mwenye kupenda kufanya maovu, na si kila mara wanapofunga makubaliano basi baadhi yao hua ni wenye kuyatupilia mbali? Huo ndio ukweli ila hakuna miongoni mwao anaeukubali. Na anapokuja kwa wao Mtume *(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam)* kutoka kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* Kuthibistisha.** *(Imam Ahmad, Imam At Tayalisi na Imam At Tabrani, Asbab Nuzul ya Aya ya 97 katika Tafsir At Tabari)*

Naam..tumeona katika Hadith ya Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* namna *Rasul Allah Salallhu Alayhi wa Salam* alivyowajibu Mayahudi kuhusiana na Chakula alichojiharamishia Nabii Yaqub, Kuhusiana Na Manii, Kuhusiana na Usingizi wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na pia kuhusiana na Malaika wake Kiongozi.

Na tunakumbushana haya kwa sababu ya kujaribu kufafanua kuhusiana na Manii, Madhii na Wadii kulingana na Mtizamo wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na namna walivyofafanua Wanazuoni ili tupate kujua ni kipi kinatengua Udhu na Kubatilisha Sala na kipi hakitengui na kwanini na Hukmu zake ni zipi katika Ibada za Dini hua Kislam ikiwemo Udhu, Sala, Funga n.k.

Ambapo kwa upande wa Manii na Madhii ambayo hutokana na chanzo cha hisia za Matamanio ya Kimwili ambapo yanapotokea hupelekea kutokea kwa Mabadiliko ya matukio yafuatayo ya Kimaumbile ndani ya mwili wa Ibn Adam iwe Mwanamme au Mwanammke.

1-Msisimko wa Mwili kutokana na Hisia za Matamanio ya Kutaka kuingiliana kimwili, kutokana na Kutizama, Kuona, Kusikia au Kuhisi kunakotokana na kupapaswa au kushikwa kushikwa kwa sehemu za Siri kunakopelekea muongezeko wa Mapigo ya Moyo, na Muongezeko wa Uzalishwaji wa Kemikali zifuatazo:

Testesterone, **ambayo ina kazi ya kuamsha msisimko wa Mwili Kimatamanio kwa Wanaume na Wanawake.**

Estrogen, **ambayo kazi yake hua ni kusimamia mzunguko wa Hedhi na pia kuuandaa Uke kwa ajili ya kuingiliana kimwili Kuurowanisha kwa Madhii na Kuutanua ndani kwa ndani.**

Dopamin, **ambayo kazi yake ni kuzalisha hisia za ari na hamu ya kutaka kuingiliana na kumsababishia mtu hisia ya Raha na kuridhika kutokana na kufikia malengo ya kuingiliana kimwili.**

Oxytocin **ambayo kazi yake hua ni kuzalisha hisia za kutaka kua na ukaribu zaidi wa kukumbatiana na kuingiliana kimwili kutokana na Kuvutiwa na kimapenzi kiuaminifu na kufurahia hali husika.**

Hivyo kuzalishwa kwa kemikali hizi hupelekea Kusimama kwa Uume kwa upande wa Wanaume ambako humpelekea Mwanamme hua na hamu ya kutaka kuujaza Uume wake kwenye Uke, na kwa upande wa Wanawake hua kututumka, kujaa na kutanuka kwa sehemu za Uke na kusimama kwa Chuchu za Maziwa kunakopelekea Mwanamke kujihisi kua Kuna haja ya ulazima wa kutaka kukumbiwa na kujazwa kitu ndani ya sehemu za Uke wake ili kutimiza mjazo wa uwazi wa mtanuko anaouhisi ndani ya Uke wake.

2-Kisha hufuatia hatua ya kuingiliana Kimwili ambako nako husababisha kuutayarisha Mwili kwa ajili ya kumwaga Manii.

3-Na kisha hatua ya tatu hua ni hatua ya kukaribia Kumwaga Manii na kunakotokana na kusikia hisia za raha kubwa sana, inayosabishiwa na kukaza kwa Misuli ya Viungo vya sehemu za Siri, kutokana na kua na hisia ya kuridhika kwa kufanikisha malengo ya kuyakinaisha Matamanio ya Mwili.

Hii ni hisia ya Raha ambayo Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhamamd Al Ghazali ameifananisha kua ni sawa na Hisia ya kuonja Ladha au Utamu wa Pepo hapa Duniani kwa mda wa sekunde kadhaa za kidunia, ambapo hali ya Raha hio kwa upande wa Peponi hua ni yenye kudumu Milele.

4-Na kisha hufuatia hatua ya Kumwaga Manii ambapo baada yake hutokea upunguaji wa nguvu za mwili na hivyo Mwili kua ni wenyekuhitajia mapumziko ya dakika kadhaa kabla kuendelea tena na kitendo cha kuingiliana kimwili.

Ambapo tunapoangalia zaidi kuhusiana na hukumu ya Manii kisharia basi tunaona kua kuna Hadith ya Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* ambae anasema kua:

سَأَلَتْ نَبِيَّ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنِ الْمَرْأَةِ تَرَى فِي مَنَامِهَا مَا يَرَى الرَّجُلُ، فَقَالَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: إِذَا رَأَتْ ذَلِكَ الْمَرْأَةُ فَلْتَغْتَسِلْ فَقَالَتْ أُمُّ سُلَيْمٍ: وَاسْتَحْيَيْتُ مِنْ ذَلِكَ، قَالَتْ: وَهَلْ يَكُونُ هَذَا؟ فَقَالَ نَبِيُّ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: نَعَمْ، فَمِنْ أَيْنَ يَكُونُ الشَّبَهُ؟ إِنَّ مَاءَ الرَّجُلِ غَلِيظٌ أَبْيَضُ، وَمَاءَ الْمَرْأَةِ رَقِيقٌ أَصْفَرُ، فَمِنْ أَيِّهِمَا عَلَا، أَوْ سَبَقَ، يَكُونُ مِنْهُ الشَّبَهُ."

Mimi nilimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Mwanamke ambae atamuota Mwanamme usingizini kama vile anavyoota Mwanamme.

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Kama Mwanammke ataota hivyo basi na Ajitoharishe.'

Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* anaendelea kusema kua: 'Mimi nilikua naona haya kuhusiana na Masuali haya, hivyo nikauliza: Jee hua inawezekana hivyo?

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Naam, kwani kama si hivyo basi itakua kuna ufanano gani? Kwani Manii ya Mwanamme na Meupe na Mazito ya Mwanamke ni Mepesi na yana Unjano njano.**

Hivyo yoyote baina yao yatakayoyazidi mengineyo au yakiwahi mwanzo kabla mengineyo basi ufanano hutokana nayo.'*(Sahih Muslim)*

Ambapo Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anasema kuhusiana na Hadith hii kua: **'Huu ndio Msingi wa Ufafanuzi wa Sifa za Manii ya Mtu mwenye Afya.'**

Na Wanazuoni wamesema kua Manii ya Mwanamme aliekua na Afya hua Meupe na mazito na hutoka kwa kuchupa na hutoka kwa Matamanio na hua ni yenye kumpa raha yanayomtoka.

Yanapotoka hufuatiwa na Harufu ya mbaali ya Maua ya Tende na harufu ya Maua ya Tende hua ni kama harufu ya Unga uliokandwa.

Na kama akiwa si Mwanamme mwenye Afya basi Manii yake hua Mepesi na yana Unjano Njano, au Mrija wa Manii huregea na Manii hutoka bila kua na Nguvu wala Kumpatia Raha anaeyatoa.

Na kama akifanya Mapenzi Sana basi hua na Wekundu kama wa Nyama, na baadhi ya Wakati hutoka kama Damu nzito.

Hivyo Sifa za Manii hua zinategemeana na Hali tatu ili yaitwe Manii. Kwanza Hutoka kutokana na Matamanio na kisha kuishiwa kwa Nguvu.

Pili hua na Harufu kama harufu ya Nyama, na ya Tatu hua ni Utokaji wake ambao ni wa Mchupo baada ya Mchupo.

Hivyo kila Moja kati ya Sifa tatu hizi hutosheleza kuthibitisha kua Yaliyotoka ni Manii, na si lazima kwa sifa zote tatu kuwepo.

Na hivyo kama Sifa tatu hizi hazitokuwepo basi haitowezekana kitu husika kuitwa Manii na hayatokua Manii. Hii ni kuhusiana na Manii ya Mwanamme.

Ama kuhusiana na Manii ya Mwanamke ambayo ni Mepesi ya njanonjano. Na Huweza kua na Weupe kulingana na Afya na Uwezo wa Mwanamke kinguvu.

Na hivyo Hua ni yenye sifa mbili ambazo ni kua na Harufu kama Manii ya Mwanamme na pili hua ni kupatikana kwa hisia za Raha na kuishiwa Nguvu baada ya kutoka kwake.*(Sharh Sahih Muslim)*

Naam..mbali ya mafunzo aliyotufafanulia Imam An Nawawi kuhusiana na Hadith hii lakini pia tunapoiangalia Hadith hii basi tunaona kua ndani yake mna Mafunzo yanayotufundisha kutoona haya kuuliza Juu ya yale tusiyoyajua hata kama mambo hayo yatakua ni yenye kutia aibu katika kuuliza kwake.

Kwani Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* alimuuliza haya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae ni Mumewe kutokana na kutaka kujua zaidi kuhusiana na Ilm ya Dini ya Kiislam na kutokana na kuuliza kwake basi ndio na sisi ikawa tunakumbushana kwa njia ya kuelimisha leo hii kuhusiana na Dini ya Kiislam.

Na kuna Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua: **'Wanawake bora ni Wanawake wa Ki Ansari (Wanawake wa Madina) Kwani Haya haikuwazuia Wao Kutokana na kutaka Kuijua na Kuifaham Dini ya Kiislam,'***(Sahih Muslim)*

Na inapokua ni kuhusiana na kufahamishana Ukweli basi hata *Allah Subhanah wa Ta'ala* amesema kua;

﴿وَٱللَّهُ لَا يَسْتَحْيِۦ مِنَ ٱلْحَقِّ﴾

Wa Allahu La Yastahyii Mina Al Haqqi*(Surat Al Ahzab 33:53)*

Tafsir: ***Na Allah si mwenye Kuona Haya juu ya ukweli***

Hivyo Hadith hii pia inatuonesha ukweli kua kama ilivyokua kwa Wanaume basi na kwa Wanawake pia hua ni wenye kuota kuhusiana na kuingiliana kimwili na Wanaume.

Hivyo Kisharia kama Mtu akiota hivyo iwe Mtu huyo ni Mwanamme au Mwanammke na kisha akaona ametokwa na Manii basi humbidi kujitoharisha kwa kukoga Janaba na hii ni Kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni kama alivyosema pia Imam An Nawawi katika Sharh Sahih Muslim.

Lakini kama ikiwa ameota hivyo lakini ikawa hakutokwa na kitu basi hua haina haja kwake kujitoharisha.

Na kama ikiwa ameamka na kujiona kua ameroa lakini hakumbuki kuota ndoto ya kiingiliana basi hukmu yake hua ni kama ifuatavyo:

Kwanza ahakikishe na kama itakua ni Manii basi hua ni Wajibu Kujitoharisha kwa kukoga Janaba na juu ya hili basi hakuna kutokukubaliana juu yake Wanazuoni, kwani imethibitishwa kama alivyosema Imam Ibn Abi Shaybah kua:

عن مالك عن إسماعيل بن أبي حكيم عن سليمان بن يسار أن عمر بن الخطاب –رضي الله تعالى عنه– غدا إلى أرضه بالجرف، فوجد في ثوبه احتلاماً، فقال: لقد ابتليت بالاحتلام منذ وليت أمر الناس، فاغتسل وغسل ما رأى في ثوبه من الاحتلام، ثم صلى بعد أن طلعت الشمس.

Amesema Malik amesema Ismail Ibn Abi Hakam kua amesema Sulayman Ibn Yasir kua Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu*altoka na kuelekea katika maeneo ya Jurf kwenye Ardhi yake na akaona Manii kwenye Nguo zake na akasema: 'Nimekumbwa na Matatizo ya kujimwagia Manii tangu nilipoanza kua Kiongozi wa Watu' na kisha akakoga Janaba, akakosha Nguo zake na kisha akasali baada ya Jua kuchomoza.*(Musanaf Ibn Abi Shaybah)*

Na amesema Imam Malik kua: **'Mtu atakaeona alam za Manii katika nguo zake, lakini akawa hajui nini kilichotokea, basi na akoge baada ya usngizi wake huo, na kama ikiwa alisali bada ya Usingizi huo basi na airudie Sala yake, kwa sababu inawezekana kua Mtu huyyo alijimwagia Manii Ndotoni bila ya yeye kujiona au amejiona lakini hakua na ndoto hio, hivyo kama akiona umaji maji kwenye Nguo zake, basi itambidi kukoga Janaba, na hii ni kwa sababu Umar aifanya hivyokwa kuirudia Sala aliyoisali baada ya kuamka kwake lakini hakurudia sala alizosali kabla ya kulala kwake.'**

Pili kama itakua ana uhakika kua Si Manii basi haina haja kwake kujitoharisha kwa kukoga bali kwa Kunawa tu na kukosha kila kilichoshikamana na Maji hayo kama ilivyo kwa Mkojo.

Tatu ni kua kama hana uhakika ni Manii ama la ana uhakika kua si Madhii kutokana hakua na Ndoto wa mawazo ya Matamanio ya Kimwili.

Basi hapa itambidi ahesabie kua hayo ni Madhii kwa sababu Madhii hua yanaweza kutoka kutokana na mawazo ya Kuingiliana kimwili na Raha inayotokana nayo na hivyo itambidi ajisafishe kwa Maji na kila kilichoguswa nayo akikoshe.

Na kama ana uhakika kua sio Manii na wala si Madhii basi hua haina haja kwake kukoga Janaba ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Mujahid Ibn Sulayman, Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi, Imam Al Hakam, Imam Hamad, Imam Malik, Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Abu Yusuf na Imam Is-haq Ibn Rahawayh.

Na hii ni kwa sababu hali ya asili ya kimaumbile huya ni Kua Tohara hivyo kutokana na kua hakuna uhakika wa juu ya Maji husika basi hua haina haja ya kujitoharisha, kwani Hakika huya haiondolewi na Shaka, lakini hata hivyo huya ni bora kukoga ili kuondoa shaka.

Ambapo kwa upande mwengine basi Imam At Tirmidhii amenukuu kutoka kwa Masahaba kadhaa wa *Rasul Allah Salallahu Alayhiwa Salam* na Tabiina miongoni mwao kama *Bahr ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Imam Ataa, Imam Al Shabi, Imam Ibrahim An Nakhai, Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad Ib Hanbal ambao wao wanasema kua Kama Mtu amejiona kua ameroa kutokana na Maji ambayo hana uhakika nayo kua ni Manii, au Madhii lakini hakumbuki kuota ndoto ya kuingiliana basi lazima akoge kama itakua alikua na sababu ya kumpelekea kutokwa na Manii kama vile kumkumbatia au kumchezea mke wake, au kufikiria kuhusiana na kuingiliana kabla ya kulala n.k.

Na kama ikiwa Mtu ameshasali na kisha akaona Maji maji kwenye nguo yake na hana uhakika na aliyoyaona kwenyenguo hizo kua ni Manii au ni Madhii, basi hua kuna njia mbili pia ambazo ni kua anaweza kuchukulia kua Maji hayo ni Manii na hivyo akakoga Janaba na kisha akasali tena upya Sala aliyoisali kabla ya kukoga Janaba.

Na pia anaweza kuichukulia kua ni Madhii na hivyo Sala yake takua ni sahih kama alisafisha Madhii hayo kutoka kwenye mwili wake na nguo yake hio na kisha akatia Udhu na kusali na nguo nyengine zilizokua Safi.

Kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: **‘Wanazuoni wetu wamesema kua kama ikiwa Mtu ameamka na amejikuta ameroa lakini hajui kama ameroa kutokana na Manii au na Madhii, na ikawa kuna uwezo wa kuchagua na mtu akaona kua bora atie Udhu na Kisha Asali huku akiwa amevaa nguo nyengine, basi Sala yake mtu huyo hua ni Sahih, na kama ikiwa atasali huku akiwa amevaa nguo ambayo imeroa bila ya kuikosha basi Sala yake hua ni batili, kwa sababu hua aidha ni mwenye kua na Janaba au ni mwenye kubeba Najsi. Hivyo kama akikoga Janaba na kusali ndani ya nguo zake hizo kabla ya kuzikosha, basi Sala yake hua ni Sahih kwa sababu ya kua kuna uwezekano ikawa kuroa huko kulikua kunatokana na Manii’***(Al Majmuu)***

Na amesema pia Aisha R*adhi Allahu Anha* kua:

سُئلَ رسولُ اللَّهِ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ عنِ الرَّجلِ يجدُ البللَ ولا يذكرُ احتلامًا ؟ قالَ : يغتسِلُ وعنِ الرَّجلِ يرَى أنَّهُ قد احتلمَ ولم يجِدْ بللًا قالَ لا غُسلَ عليهِ قالت أمُّ سلمةَ يا رسولَ اللَّهِ هل علَى المرأةِ ترَى ذلِكَ غُسلٌ قالَ نعَم إنَّ النِّساءَ شقائقُ الرِّجالِ.

‘***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **aliulizwa kuhusiana na Mtu aliona unyevunyevu kwenye Mwili wake na Nguo zake, lakini hakua ni mwenye kukumbuka Kuota kuhusiana na Kuingiliana kimwili.**

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: ‘Inambidi Mtu huyo Kukoga.’

Na akaulizwa tena kuhusiana na Mtu ambae anakumbuka kua aliota Ndoto ya kuingiliana ndani yake lakini Hakujikuta kua ameroa.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Haimlazimu Mtu huyo Kukoga.'**

Na kisha Ummu Salamah akauliza: 'Je na Mwanamke akiona hivyo hua ni Wajibu kukoga pia?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama*akasema: 'Naam, Wanawake ni wenza wa Wanaume.'** *(Sunnan Abu Daud)*

Ambapo tumesema kua hukmu ya mtu kama huyu hua ni kukoga huko hua ni kukoga Janaba. Ambapo neno Janabah kwa Kilugha hua linamaamisha Kugeuka, Kuweka Upande,Kuepusha,Kuweka Kando, kuweka Mbali, Kukataa Kitu, Kukaa mbali na Kitu.

Neno Janabah ndio lililotoa neno *Junub* ambalo humaanisha Mtu Mgeni, Mtu wa Mbali na pia humaanisha Mtu ambae anatakiwa kujitoharisha kwa Kukoga.

Hivyo Mtu mwenye Janaba humaanisha kua Mtu ambae yuko Mbali na Ibada kutokana na kua ni mwenye kua katika hali ya Kuingiliana Kimwili na hivyo anawajibika kukoga kabla ya chochote. Na hivyo ingawa Mtu huyo hua haruhusiki kuingia kwenye Ibada hadi atieudhu na kisha akoge lakini hata hivyo Mtu huyo hua si Najis, na hii ni kwa Sababu Muislam hawezi kua Najis kwa sababu neno Najis hua linamaanisha Kutokua na Usafi wa Kimwili na Kiakili kutokana na kujaa Uchafu.

Kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika hadith ifatayo:

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، قَالَ حَدَّثَنَا يَحْيَى، قَالَ حَدَّثَنَا حُمَيْدٌ، قَالَ حَدَّثَنَا بَكْرٌ، عَنْ أَبِي رَافِعٍ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم لَقِيَهُ فِي بَعْضِ طَرِيقِ الْمَدِينَةِ وَهْوَ جُنُبٌ، فَانْخَنَسْتُ مِنْهُ، فَذَهَبَ فَاغْتَسَلَ، ثُمَّ جَاءَ فَقَالَ " أَيْنَ كُنْتَ يَا أَبَا هُرَيْرَةَ ". قَالَ كُنْتُ جُنُبًا، فَكَرِهْتُ أَنْ أُجَالِسَكَ وَأَنَا عَلَى غَيْرِ طَهَارَةٍ. فَقَالَ " سُبْحَانَ اللَّهِ، إِنَّ الْمُؤْمِنَ لاَ يَنْجُسُ "

Amesema Aliyu Ibn Abd Allahi kua amesema Yahya kua amesema Humayd ku amesema Bakru kua amesema Abi Rafii kua Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikutana na mimi katika Moja kati ya Mitaa ya Madina huku mimi nikiwa na Janaba.

Hivyo nikamchomoka na kuenda kukoga na kisha nikarudi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na nilipofika basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Ewe Abu Hurayrah Ulikua wapi?'

Hivyo nami nikajibu kwa kusema *Ya Rasul Allah* Mimi nilikua na Janaba hivyo sikupenda kukaa pamoja nawe.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema:'Subhanah Allah! Muumini kamwe hawezi kua Najis.**'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo Imam An Nawawi amesema kuhusiana na Hadith hii kua: **'Hadith hii ndio Msingi Mkuu wa Kua Muislam hawezi kua Najis iwe Muislam huyo yuko hai au amekufa**

Ambapo Kuhusiana na Usafi wa Muislam aliehai basi kuna Makubaliano ya Wanazuoni Juu yake Lakini kuhusiana na usafi wa Maiti wa Kiislam basi Wanazuoni wametofautiana Juu yake lakini mtizamo unaokubalika zaidi ni kua hua Msafi na ndio maana hua anatakiwa Kukoshwa

Ila kuhusiana na Wasiokua Waislam basi nao Usafi wao wa Mwili hua ni kama wa Waislam na huu ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na wengi Miongoni mwa Wanazuoni waliotangulia. Ambapo kuhusiana na ile aya isemayo kua:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُواْ ٱلْمَسْجِدَ ٱلْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَٰذَا وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ ٱللَّهُ مِن فَضْلِهِ إِن شَآءَ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo innama almushrikoona najasun fala yaqraboo almasjida alharama baAAda AAamihim hadha wa-in khiftum AAaylatan fasawfa yughneekumu Allahu min fadlihi in shaa inna Allaha AAaleemun hakeemun.*(Surat At Tawbah 9:28)*

Tafsir: ***Enyi Mlioamini kwa hakika Washirikina Ni Najis hivyo msiwaruhusu kukaribia Masjid Al Haram baada ya mwaka huu, na kama mtakua mnakhofia Umasikini basi Allah Atakutajirisheni akitaka kutokana na Neema zake kwani kwa hakika Allah ni mwenye Kujua juu ya kila kitu na ni mwenye wingi wa Hikma.***

Basi Najis hii yao wao iliyozungumziwa hapa ni Najis ya Kiimani na hivyo hua hawahesabiki kua ni Najis kama Mkojo au Kinyesi n.k.*(Sharh Sahih Muslim)*

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِّنَ ٱلطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلاً﴾

Walaqad karramna banee adama wahamalnahum fee albarri waalbahri warazaqnahum mina alttayyibati wafadhdhalnahum AAala katheerin mimman khalaqna tafdheelan. *(Surat Al Isra 17:70)*

Tafsir: ***Na kwa hakika tumemkirimu na kumheshimisha Bani Adam. Na tukambeba yeye juu ya Ardhi na Juu ya Bahari na kumruzuku kwa viliyo vizuri na vya halali na tumewapendelea wao juu zaidi ya wale tuliowaumba kwa upendeleo Mkubwa sana.***

Hivyo Wanazuoni Wanasema Vitu vitatu havikujumuishwa katika Nyama ambayo ni Najis ambavyo ni:

Kwanza ni Maiti ya Ibn Adam kwani Wamepandishwa Darja na *Allah Subhanh wa Ta'ala* wakiwa hai au wamekufa ambapo amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

المسلم لا ينجس حياً وميتا

Muislam hawi Najis iwe awe hai au maiti.

Pili na Tatu ni Samaki na Nzige kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua

"أحلت لكم ميتتان ودمّان، فأما الميتتان فالحوت والجراد، وأما الدمان فالكبد والطحال

Maiti wa Aina Mbili ni Halali kwenye na Damu za aina Mbili ni Halali kwenu. Maiti mbili ni Samaki na Nzige na Damu mbili ni Ini na Figo*((Imam Ibn Majah)Fiqh Manhaj Ala Madhhab Al Imam Al Shafii)*

Hivyo Aya na Hadith zinaturudisha katika kufafanua kwa nini Manii ikawa Si Najis. Ambapo juu ya suali hili basi kuna kutofautiana kidogo kwani kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi wao wanasema kua: **'Manii ni Najis.'**

Kama anavyosema Imam Abd Allah Ibn Mahmud Al Mawsil Al Hanafi kua:'**Kitu chochote kitakachotoka nje ya mwili wa Ibn Adam ambacho kitampelekea Mtu kutakiwa Kujitoharisha hua ni Najis**. **Kwa mfano kama Choo kikubwa, Mkojo, Damu,Usaha, na Matapishi na hakuna kutofautiana juu ya hili. Na hili pia ni kuhusiana na Manii kama vile *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomwambia Aisha *Radhi Allahu Anha* kua:** '**Kama ikiwa hayajakauka basi kosha na kama ikiwa yamekauka basi yatoe kwa kuyakwangua kutoka katika Nguo Na pia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimwambia Amar Ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* kuaNguo inatakiwa ikoshe kutokana na Manii, Mkojo na Damu.**

Na kama Manii yakikaukia kwenye Mwili basi Al Hasan amenukuu kutoka kwa Imam Abu Hanifa kua Mwili haui Tohara kwa Kuyakwangua.

Lakini hata hivyo Al Kharki amenukuu pia kutoka kwa Wanazuoni wetu kua Mwili unakua Tohara, na hii ni kwa sababu hili ni jambo ambalo linatokea mara kwa mara. Na hivyo hua ni vigumu kuliepuka, ambapo hata hivyo kuyakwangua hakumaanishi kua Manii ni Masafi, kwani kulingana na mtizamo sahih wa Imam Abu Hanifa basi ni kua Manii hua yanapungua unapoyakwangua kwenye nguo na hivyo hua inaruhusika kusali katika hali kama hio.' *(Al Ikhtiyar Lil Taalil Al Mukhtar)*

Na akasema Imam Akmal Ad Din Muhammad Ibn Muhammad Ma Babarti Al Hanafi kua: **'Manii ni Najis na kuyapangusa tu pale yanapokua yamekauka hutosheleza na yanapokua mabichi basi inabidi nguo kukoshwa'***(Al Inaya Sharh Al Hidaya)*

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi Anasema Imam Al Dardir Al Maliki kua: '**Miongoni mwa vitu ambavto ni Najis ni pamoja na Manii, Madhii, na Madii hata kama yakiwa yanatokana**

na vyanzo ambavyo ni halali kuvila katika vitu vyote vitatu hivi. Na hii ni kutokana na hali yake ya Kukirihisha vitu hivyo kimaumbile na kua vinaweza kugeuka na kua Najis, na pia kwa sababu vitu hivi asili yake hua ni Damu, na hivyo kusamehewa kwa asili yake basi haimaanishi kua navyo vimesamehewa pia.' *(Sharh Al Kabir Al Dardir)*

Hivyvo mbali ya kua kulingana na mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii ni kua:**'Kila kitu kitakachotoka katika Uume iwe Mkojo, Madhii, Wadii au Kitu chengine kisichojulikana basi Hukmu yake ni kua kitu hicho ni Najis Isipokua Manii.'***(Al Umm).*

Ambapo juu ya suali hili basi kuna kutofautiana kidogo kwani kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi wao wanasema kua: Manii ni Najiskama tulivyoona kutoka kwa Wanazuoni wao.

Na tunaporudi kwa upande wa Madhhab ya Imm Al Shafii basi tunaona kua: '**Anasema Shaykh Ul Islami Al Hafidh, Al Shaykhan Hujjat Ul Islami Imam Ad Din Imam Abd Al Karim Ibn Muhammad Ibn Abd Al Karim Ibn Fadhl Ibn Husein Ibn Hasan Abu Qasim Al Rafii Al Qazwini Al Shafii kua:Ama kuhusiana na Manii ya Ibn Adam basi ni Tohara.'**

Na hii ni kutokana na Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua: Nilikua Nikifuta Manii kwenye Nguo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha yeye alikua Akisalia Nguo hio*((Sahih Muslim) Al Aziz Sharh Al Wajiz)*

Ambapo huu Mtizamo wa kua Manii ni Tohara ambao ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ndio pia Mtizamo wa Masahab kina Saad Ibn Abi Waqqas, Abd Allah Ibn Umar, Aisha *Radhi Allahu Anhum.*Na kwa upande wa Maimamu basi ndio Mtizamo wa Imam Sayyid Ibn Musayyib, Imam Ataa, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Thawr, Imam Abu Daud, Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri na Imam Ahmad Ibn Hanbal na Madhhab yake.Ambapo katika kutaja jina lake Imam Al Rafii basi tumetaja cheo cha Shaykhan yaani Mashaykh Wawili.

Naam..hiki ni cheo Ambacho kinabebwa na Wanazuoni wawili wakuu wa Fatwa katika Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ni Imam Al Rafii na Imam An Nawawi.Kwani Maimamu Wawili hawa ndio waliofanya kazi ya Kufafanua kitabu cha Fiqh cha 3 cha Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii kiitwacho Al Wajiz ambacho kutokana nacho basi Imam Al Rafii alitoa vitabu vitatu ambavyo ni Sharh Al Saghir Fath Al Aziz Fi Sharh Al Wajiz, na Sharh Kabir yake na kiaha akatoa Al Muharrar na kisha Imam An Nawawi akaifafanua Al Muharrar kwa kitabu cha Minahji Talibin na akaifafanua Aharh Al Kabir hio ya Imam Al Rafii kwa kutoa kitabu kiitwacho Rawdhat Talibin. Na Hii ni mada nyengine ambayo inapatikana katika cha Al Mustakshif Abu Manal Danah kiitwacho Ijtihad na Taqlid Histoaria Ya Maimamu na Madhhab yao Katika Uislam ambacho kinapatikana bure Mtandaoni kwa anaetaka.

Hivyo tunapomuangalia Shaykhan mwenza wake Imam Al Rafii yaani Imam An Nawawi basi tunaona kua yeye anasema kuhusiana na Utohara wa Manii kua:'**Manii ya Ibn Adam ni Masafi kulingana na Mtizamo wetu sisi Mashafii, na huu ndio Mtizamo sahih kama ilivyoelezewa na Al Shafii Mwenyewe katika vitabu vyake**. **Na huu pia ndio Mtizamo wa wengi sana Miongoni mwa Wanazuoni, ambapo muandishi wa Al Bayan (Imam Imran Al Shafii) amenukuu mitazamo miwili juu ya kutokua Tohara na kisha akasema:** '**Kama tukisema ku ni Tohara basi hua inapendekezwa kuyakosha kutoka kwenye Mwili na kwenye Nguo na hii ni kulingana na hadith sahih zilizomo kwenye Bukhari na Muslim. Kutoka kwa Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua alikua akikosha Manii kutoka kwenye nguo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Na hii inaondoa Utata wa kutokukubaliana kwa Wanazuoni kuhusiana na Utohara wake. **Na Mtizamo wa kua Manii ni Tohara ni mtizamo pia wa Said Ibn Musayib, Ataa, Is-haq, Abu Thawr, Daud, na Ibn Al Mundhiri amesema kua ni Tohara na huu ndio Mtizamo sahih zaidi baina ya Mitizamo miwili ya Ahmad Ibn Hanbal**. **Ambapo Abu Hanifa, Malik, Al Thawry na Al Awzai wanasema kua si Tohara**. **Na Abu Hanifa amesema kua inatosheleza kuyapangusa tu lakini Al Awzai na Malik wamesema kua inabidiyakoshwe.'***(Al Majmuu)*

Ama kwa upande wa Imam Abu Bakr Al Bakri Uthman Ibn Shatta Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Amesema Imam Al Bujaraimi kua Al Shafii na Ahmad wamesema kua Manii ni Tohara, na Al Shafii ameongezea kwa kusema kua:Hata Manii ya Mnyama aliekua halali kuliwa hua ni Tohara***(Ianat Talibin Aala Hal Al Fadhl Fath Al Muin)*

Ambapo amesema Muwaffaqah Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua:'**Ingawa tunasema kua Manii ni Tohara lakini hua ni bora kuyapangusa kutoka kwenye nguo, ila kama mtu akisali bila ya kuyafuta Basi Sala yake hua Sahih.'** *(Al Mughni)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Wale wanaosema kua Manii si Tohara basi wao wamenukuu hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambayo amesema kua alikua akikosha kwa kutia Maji nguo yenye Manii ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* kama ilivyonukuliwa na Muslim Na pia katika Hadith nyengine pale aliposema kua Nilikua Nikiyakosha kutoka katika Nguo ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* ambayo imenukuliwa na Bukhari na Muslim.**

Na katika Hadith ya Muslim basi Aisha *Radhi Allahu Anha* amesema kumwambia Mtu ambae aliifua kabisa nguo yake yote baada ya kua na Manii kwa kusema kua: 'I**ngetosheleza kwako wewe baada ya kugundua Mabaka ya Manij kwa kukosha katika sehemu husika tu,na kama hukuona basi ungerashia rashi maji tu pembeni yake.Kwani mimi nilikua nikiyapangusa kutoka katika Nguo ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha nae aliisalia Nguo hio.**

Hivyo As-hab wetu (wa Madhhab ya Imam Al Shafii) Basi wao wamenukuu hadith ya Kuyapangusa Manii kua uthibitisho wa kua kama Manii yangekua si Tohara basi isingetosheleza kuyapangusa, kama vile ilivyokua kwa Damu, Madhii na mengineyo. **Hivyo uthibitisho huu unatosheleza na ndio ninaoutegemea kuhusiana na Usafi na Utohara wa Manii.'***(Al Majmuu)*

Kisha Imam An Nawawi akasema tena kua: 'Mwandishi wa Al Bayyan na Wanazuoni wa Khurasan wamenukuu mitizamo miwili kuhusiana na kua Manii sio Tohara Ambapo miongoni mwao mitizamo miwili hio basi ni usemao kuhusiana na Manii ya Mwanamke kua pia si Tohara Lakini Mtizamo sahih kabisa ni kua Aina zote za Manii ni Tohara iwe ya Mwanamme au ya Mwanamke, iwe Muislam iwe si Muislam.'*(Al Majmuu)*

Ambapo tunaporudi kwa Imam Ad Din Imam Abd Karim Ibn Muhammad Al Rafii Al Shafii basi nae anaendelea kutuambia kua: '**Pale itakapokua Manii si ya Ibn Adam bali ya Mnyama mwengine basi Mtu anatakiwa aangalie, kua kama Mnyama huyo ni Najis basi na Manii yake pia yatakua ni Najis, na kama Mnyama huyo atakua ni Tohara basi juu yake kuna Mitizamo mitatu ifuatayo:**

1-Mtizamo unaokubalika kwa vithibitsho zaidi ni kua Manii ya Mnyama huyo yatakua si Tohara.

Na hii ni Kutokana na kua Manii hubadilikia ndani ya mwili kama vile ifanyavyo Damu,na hivyo hua ni Tohara kwa upande wa Ibn Adam tu na ni kwa sababu ya Kuheshimishwa kwao na *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

2-Kua ni Tohara na hii ni kwa sababu ya Asili ya Utohara wa Mnyama Husika na hivyo hua ni sawa na Manii ya Ibn Adam.

3-Kua Ni Tohara lakini kwa Mnyama anaeliwa na si Tohara kwa Mnyama ambae ni Haram kummla kama vile ilivyokua kwa Maziwa ya Wanyama husika.' *(Al Aziz Sharh Al Wasit)*

Na kwa upande wa Imam An Nawawi amefafanua zaid Ufafanuzi huu wa Imam Al Rafii katika Al Aziz Ala Sharh Al Wasit kutoka kwenye kitabu cha Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii cha Al Wasit. Hivyo Imam An Nawawi anafafanua katika Minhaj Talibin kwa kusema kua: **'Hivyo mtizamo unaokubalika zaidi kuhusiana na Manii basi ni kua ya Wanyama wote ni Tohara isipokua ya Mbwa, Nguruwe na Vizazi vya kama hao.'***(Minhaj Talibin)*

Na kisha akasema tena Imam An Nawawi katika Rawdhah Talibin kua: **'Mimi nnasema kua Mtizamo Sahih kulingana na Wanazuoni wetu wa As-hab Al Wujuh (Wanazuoni wathibitishaji wa Fiqh ya Madhab ya Imam Al Shafii) na Wanazuoni wengineo basi ni kua Manii ya Wanyama wengineo isipokua ya Mbwa, Nguruwe na Vizazi vyao kua ni Tohara, na Allahu Aalam.'***(Rawdhah Talibin)*

Hivyo Ingawa Imam Abu Hanifa na Imam Malik Wanasema kua Manii Ni Najis Na Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Hanbal basi ni kua: '**Manii ni Tohara. Lakini wote wanakubaliana kua yatakapokutoka kama una Udhu basi utatenguka na hivyo kama ulikua ndani ya Sala basi Sala nayo itabatilika na Itakubidi Kukoga Janaba kabla Kusali. Kwani Amesema Yahya Ibn Abd Rahman Ibn Hatib kua:**

((أنَّ عمر رضي الله عنه أصابته جنابة وهو في سفر، فلما أصبح قال: أَتَرَوْنا ندرك الماء قبل طلوع الشمس؟ قالوا: نعم، فأسرع السير حتى أدرك فاغتسل، وجعل يغسل ما رأى من الجنابة في ثوبه، فقال عمرو بن العاص رضي الله عنه: لو لبست ثوبًا غير هذا وصليت؟ فقال له عمر رضي الله عنه: إن وجدت ثوبًا وجده كل إنسان؛ إنِّي لو فعلت لكانت سُنَّة، ولكني أغسل ما رأيت، وأنضح ما لم أرَه)

'Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alikosa Tohara wakati tukiwa Safarini.

Na hivyo Alfajir ilipoingia akasema: Hivi Jee mnafikiria kua tunaweza tukapata sehemu yenye Maji kabla ya Kuchomoza Jua?

Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakasema: Naam!

Hivyo tukahatakisha kutembea hadi tukakuta Maji, na kisha Akakoga Janaba na kukosha Manii aliyoyaona kwenye Nguo yake.

Ambapo Amr Ibn Al A'as *Radhi Allahu Anhu* akasema: Kwanini Usivae nguo Nyengine Badala yake Na kissha Ukasali?.

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Kama ningepata Nguo Nyengine basi na kila Mtu ingembidi kutafuta nyengine, Hivyo mimi Nimekosha kile nilichokiona na nisichokiona basi nimekirashia rashia maji.' *(Muwwata Imam Malik, Musanad Imam Abd Razak, Imam Tahawi katika Sharh Maani Al Athari)*

Na akasema Zayd Ibn Salt kua:

((خرجت مع عمر بن الخطاب رضي الله عنه إلى الجرف، فنظر، فإذا هو قد احتلم، وصلى ولم يغتسل، فقال: والله ما أراني إلا احتلمت وما شعرت، وصليت وما اغتسلت، قال: فاغتسل، وغسل ما رأى في ثوبه، ونضح ما لم يَرَ، وأذَّن أو أقام، ثم صلى بعد ارتفاع الضحى متمكنًا))

'Nilienda Safari katika maeneo ya Jurf pamoja na Umar Ibn Al *Khattan Radhi Allahu Anhu.* Na akasali na kisha akajiona kua Nguo yake ina Manii na hivyo na akagundua kua alisali bila ya kukoga Janaba, hivyo akasema:

WaAllahi! Nadhani kua Niliota na Kujimwagia bila kujijua na hivyo nimesali bila ya Kukoga Janaba.

Hivyo akakoga Janaba na kisha akakosha kile alichokiona kwenye Nguo yake na kile ambacho hakukiona akakirashia rashia Maji, na kisha Aliadhini au Alikimu Sala na Kisha akasali katika Mda ambao imeshapita Salat Dhuha.' *(Malik Muwwata, Musanaf Imam Ibn Shaybah, Musannaf Ibn Abd Razzaq)*

Ambapo hadith hii hii tena imenukuliwa na Al Sharid *Radhi Allahu Anhu,* na Mujaddid Ad Din Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri amesema kua hii ni Hadith Sahih.

Na amesema Khalid Ibn Abi Uzza kua:

((سأل رجل عمر بن الخطاب رضي الله عنه فقال: إنِّي احتلمت على طنفسة؟ فقال: إن كان رطبًا فاغسله، وإن كان يابسًا فاحْكُكْهُ، وإن خفيَ عليك فارْشُشْه))

'Kuna Mtu alimuuliza Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema kua: Mimi nimeota na nikajimwagia Manii kwenye Mkeka.

Ambapo Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema kua: Kama Ni Mabichi basi yakoshe, na kama yameshakuka basi yakwangure, na kama hujui ni wapi basi rashia rashia Maji tu.' *(Musannaf Ibn Abi Shaybah)*

Ambapo amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua:

((إن خفيَ عليه مكانه وعلم أنَّه قد أصابه، غسل الثوب كله))

‘**Kama ikiwa Mtu hajui Sehemu yalipomwagikia Manii kwenye Nguo yake basi itambidi aikoshe Nguo nzima.’** ***(Musannaf Ibn Abd Razaq, Ibn Abi Shaybah)***

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

((إذا علمت أنْ قد احتلمتَ في ثوبك، ولم تدرِ أين هو، فاغسل الثوب

‘Kama ikiwa Mtu unajua kua una Manii kwenye Nguo yako, na hujui yako wapi basi basi ikoshe nguo yote,na kama huna uhakika kama imeingia nguo hio Manii ama la basi irashie rashie Maji.’ ***(Musannaf Ibn Abi Shaybah, Ibn Abi Razaq)***

Ambapo hizo ni baadhi ya Hadith zinazotumiwa kama Vithibitisho kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik. Na kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanatumia Vithibitisho vifuatavyo:

Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

(إذا احتلمت في ثوبك فأمِطْه بإذْخِرة أو خِرْقة، ولا تغسله إن شئت إلا أن تقذره أو تكره أن يُرى في ثوبك)

‘Kama ikiwa Mtu atajimwagia Manii kwenye Nguo yake basi pangusa kwa Kitambaa na haina haja ya kukosha Nguo kama hutaki isipokua kama utaona kua inakukirihisha kwenye Nguo.’*(Musanaf Ibn Abd Razaq, Al Umm Imam Al Shafii, Sunan Ad Daraqutni na Imam At Tahawi katika Sharh Maani Al Athar)*

Ambapo Imam Al Bayhaqi basi yeye amesema kua inakua kama Mafua au Mate ya Mtu kwenye Nguo.

Na amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

(أربع لا تنجس – وعند الدارقطني: لا يجنبن – الأرض، والثوب، والماء، والإنسان)

‘Vitu vinne havimfanyi Mtu Kutengukwa na Udhu: Ardhi, Nguo, Maji na Mtu*(Sunan Ad Daraqutni n Tadhhib Al Athar Imam At Tabari)*

Na akasema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abas *Radhi Allahu Anhu* kua:

إذا أجنب الرجل في ثوبه فرأى فيه أثرًا فليغسله، وإن لم ير فيه أثرًا فلينضحه

‘Kama Mtu aakitokwa na Manii na akaona Manii kwenye Nguo zake basi na Akoshe na kama haoni basi na arashie rashie Maji.’ *(Musanaf Ibn Abi Shaiba, Ibn Abd Razaq)*

Na anasema Abd Allah Ibn Shihab Al Khawlani kua:

((كنت نازلًا على عائشة رضي الله عنها فاحتلمت في ثوبي فغمستهما في الماء، فرأتني جارية لعائشة فأخبرتها فبعثت إليَّ عائشة رضي الله عنها فقالت: ما حملك على ما صنعت بثوبيك؟ قال قلت: رأيت ما يرى النائم في منامه، قالت: هل رأيت فيهما شيئًا؟ قلت: لا، قالت: فلو رأيت شيئًا غسلته؟ لقد رأيتني وإنِّي لأحكُّه من ثوب رسول الله صلى الله عليه وسلم يابسًا بظفري))؛

‘Mimi nilikua nakaa kwenye Nyumba ya Aisha *Radhi Allahu Anha,* na hivyo Usiku Nikaota na Kujimwagia na asubuhi nikaitumbukiza kwenye Maji nguo yangu hio

Ambapo mfanyakazi wa Aisha *Radhi Allahu Anha* akaniona na kumtaarifu Aisha *Radhi Allahu Anha* ambapo nae akaniita na akaniuliza

Hivi ni kitu gani kilichokupelekea wewe kufanya uliyoyafanyia Nguo yako?

Nami nikasema: ‘Mimi niliota yale yanayotwa ndani ya Ndoto.’

Nae akaniuliza: ‘Jee umeona kitu chochote kile kwenye nguo zako?’

Nami nikasema ‘La!’

Ambapo nae akasema: ‘Kama ingekua Umeona kitu basi ndio Ungeikosha? Wakati mimi nilikua nikiyawangura kwa kucha zangu yalipokua yamekaukia kwenye nguo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.’*(Sahih Muslim)*

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: ‘**Wanazuoni wanakubaliana kua Kama Manii yakimtoka Mtu basi Mtu huyo huwajibika Kukoga Janaba Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi haijaalishi kama Manii hayo yalitoka kaa Kuingiliana Kimwili, Kwa Kuota Ndoto, Kujipapasa ama la, Kwa Matamanio ama la, kwa kuangalia ama la, Mengi au Kidogo au Kitone kimoja tu**. **Iwe mtu huyo amelala au yumacho awe Mwanamme au Mwanammke awe na akili au hana akili, basi hali zote hizi humuwajibishia Mtu kukoga Janaba na hii ni Kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu ya Al Shafii.**

Ama kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Malik na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: ‘Kama Manii yatatoka kwa Nguvu na Matamanio basi hapo ndio humuwajibisha Mhusika kukoga Janaba kama ilivyoelekezwa na Hadith Sahih.’

‘Na Manii Yakiwa Mabichi basi hua na harufu ya Weupe wa Mayai na yakikauka hua na Harufu ya Unga Uliokandwa’*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Ambapo amesema Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Naqib Al Masri Al Shafii kua:**‘Manii Yakiwa Mabichi basi hua na harufu ya Weupe wa Mayai na yakikauka hua na Harufu ya Unga Uliokandwa’** *(Umdat Al Salik wa Uddat Al Nasik)*

Ambapo anasema Imam Ahmad Ibn Ahmad Al Adawi Al Maliki Ad Dardir kua: ‘**Kama Mtu yatamtoka Manii baada ya Matamanio ya kawaida tu bila ya kuingiliana kimwili, yaani kwa**

kuangalia tu, kufikiria au Kupapasa, na akatokwa nayo wakati huo huo Au Baadae baada ya kumalizika ladha na msisimko basi hatowajibika kukoga Janaba, kwani Wajibu wa Kukoga Janaba kutokana na Manii hua ni Kutokana na Kutoka kwa Matamanio ya Kuingiliana Kimwili na sio kutoka nje tu.'*(Sharh Al Kabir)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Khalil Ibn Is-haq Al Jundi Al Maliki basi anasema kua: '**Ni Wajibu Kukoga Janaba baada ya Kutokwa na Manii hata kama ikiwa yametoka kutokana na Ndoto au mda baada ya Matamanio bila kuingiliana**.' *(Mukhtasar Al Khaili)*

Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Sahal Abu Bakr Al Sarakhasi Al Hanafi basi yeye amesema kua: '**Kama Ikiwa Mtu ataota Ndoto ya Matamanio lakini akayazuia Manii yasimtoke hadi pale baada ya kumalizika Ladha ya Matamanio na Msisimiko na kisha yakamtoka, basi Mtu huyo humuwajibikia Kukoga Janaba.'***(Al Mabsut)*

Na kwa upande wa Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi basi anasema kua: '**Ama kuhusiana na Mtizamo wa Ahmad Ibn Hanbal basi ni wenye kujulikana kwani aliulizwa kuhusiana na Mtu ambae alilala na akaota akiwa anaingiliana kimwili, na kisha alipoamka akawa hakuona Dalili ya kutokwa na Manii. Hivyo akanyanyuka na alipotoka tu kitandani basi Manii yakamtoka, Jee afanyeje? Imam Ahmad Ibn Hanbal akasema kua: Anawajibika Kukoga Janaba.'***(Al Mughni)*

Na kwa upande wa Al Muhaqqiq Al Alamah Imam Muhammad Amin Ibn Amar Ibn Abd Al Aziz Ibn Ahmad Ibn Abd Rahman Ibn Najmu Ad Din Ibn Aabidin Al Shami Al Hanafi basi anasema kua: '**Ili Manii yamwajibishe Mtu kukoga Janaba basi yanatakiwa yawe ni yenye kuenda sambamba na Ladha na Msisimko wa Matamanio (Shah-wah) tangu mwanzoni mwa kutoka kwenye chanzo chake ndani ya Mwili.**

Hivyo hali hii inapotokea na kusimamia kwenye Msingi wa kumwagwa kwake nje kutoka katika sehemu za Siri basi hapo ndio itawajibika Kukoga Janaba. Kwani kulingana na Mtizamo wenye Nguvu kwenye Madhhab yetu (ya Abu Hanifa) basi Kutoka kwa Nguvu kwa Manii hua si sharti pale inapokua asili ya utokaji wake haitokani na Msisimko wa Matamanio na Kujiridhisha. Hivyo katika hali ya Msisimko na Matamanio kama Manii yatabakia na baada ya Mtu kukoga Janaba Na hapo hapo yakamtoka basi hii humpelekea Mtu husika kurudia Upya Kukoga Janaba.

Ila kama ikiwa yatamtoka baada ya Kulala, Kutembea, Kukojoa mda baada ya Kukoga Janaba, basi katika hali kama hii hatowajibika kukoga Janaba, kwa sababu hayakutoka kwa Msisimko wala Matamanio.' *(Radd Al Mukhtar)*

Na Amesema Muadh ibn Muadh kua amesema Iqrimah Ibn Amar kua amesema Ubay Allah Ibn Ubayd kua Aisha *Radhi Allahu Anha* kua:

كان رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ يَسلُتُ المنيَّ مِن ثَوبِه بعِرْقِ الإذْخِرِ، ثم يُصلِّي فيه، ويَحُتُّه مِن ثَوبِه يابِسًا، ثم يُصلِّي فيه.

'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **alikua akipangusa Manii kutoka kwenye Nguo yake kwa Mzizi wa Mti wa Idhkir, na kisha husali huku akiwa ameivaa nguo hio. Na pia alikua akiyakwangua Yanapokua Yamekaukia kwenye Nguo Yake na kisha Husali na Nguo hio***.'(Musnad Imam Ahmad)*

Na amesema **Imam Is-haq Ibn Rahawayh kua amesema Nadir Ibn Shumayl kua amesema Iqrimah Ibn Amar Al Yamani kua amesema Abd Allah Ibn Ubayd Ibn Umar kua amesema Aisha Radhi Allahu Anha kua: Nimemuona mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiyapangusa Manii kwenye Nguo yake kwa Mzizi wa Idhkir na alipokua akiyaona yamekauka Nilimuona akiwa anakwangua na kisha Kusalia Nguo hio.'***(Musnad Imam Is-haq Ibn Rahawayh)***

Na amesema Imam At Tirmidhii kua: **'Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:**

سئل رسول الله صلى الله عليه وسلم عن المني يصيب الثوب، قال "إنما هو بمنزلة المخاط والبزاق والبصاق"، وقال:"إنما يكفيك أن تمسحه بخرقة أو إذخرة"

Aliulizwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kuhusiana* na Manii kwenye Nguo, ambapo nae akajibu kwa kusema: Manii ni Kama Mafua, hivyo Jipanguseni hata kama kwa Idhkir.'*(Imam At Tirmidhi, Imam Ad Daraqutni, Imam Al Bayhaqi)*

Ambapo Idhikir ni Mti ambao una Majani mapana yenye harufu kama ya Mlimau, na Maua yake hutumika kama kiungo cha Chai.

Ambapo amesema Imam Abu Isa Al Tirmdhii kua: '**Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* isemayo kua alikua akikosha Manii kutoka kwenye Nguo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,*haipingani na Hadith ya Kupangusa Nguo kutokana nayo na hii ni kwa sababu, hata kama Kupangusa kutatosheleza basi hua inapendekezwa kua Mtu asionekane Mtu akiwa Na amegandwa na Manii.'**

Na amesema Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Hakuna kupingana baina ya Hadith ya Kukosha na Hadith ya Kupangusa kwa sababu kuzichanganya Hadith hizi mbili hua ni bora zaidi kwani ziweka wazi juu ya Mtizamo wa Utohara wa Manii, na kutoa Hukmu ya kua inapendekezwa Kukosha kwa ajili ya Kusafisha na hivyo Kukosha hua si Wajibu. Na huo ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii na Imam Ahmad pia na Wanazuoni wa Hadith ambao wamesema kua Manii ni Tohara. Na pia kujumuisha kwa pamoja pia inakubalika pale tukichukulia kuhusiana na Mtizamo wa kua si Tohara kwa Kukosha Nguo pale yatakapokua Mabichi na Kukwangua pale yatakapokua Yamekauka.***'(Fat-h Al Barr)***

'Kwa upande wa Mtizamo wa Mahanafi wanasema kua Manii Ni Najis, ambapo hua inatosheleza Kuondoa Unajis wake kama tukichukulia kua Kukosha hua ni kwa kitu kilichokua na Maji na Kukwangua kwa kitu Kikavu kama vile Kiatu kinaposafika kutokana na Kukwaruzwa na Udongo na kulingana na Mtizamo wao pia ni kua Jua Huitoharisha Ardhi na hivyl hua hakuna haja ya kuikosha Ardhi. **Ambapo kwa Upande wa Malik basi wao wanasema kua Kukosha Nguo yenye Manii hua ni Wajibu kwa hali yeyote ile yatakavyo kua, kwani Kukwangua wala kupangusa hua hakutoshelezi**.'***(Kitab Sharh Sunan At Tirmidhii)***

Hivyo kulingana Na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi ni kua Manii ni Tohara na hivyo hata kama yakiingia kwenye Nguo yako, basi nguo basi Nguo hio hua Tohara na hata kama Mtu akiisalia Nguo hio basi Sala yake haibatiliki.

Ambapo anasema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Ijapokua Tunasema kua Manii ni Tohara, lakini hua ni bora kuyapangusa kuliko kuyaachia kama yalivyo,**

lakini kama Mtu akisali Na Nguo zilizoingia Manii bila ya Kuyafuta basi hua hamna Tatizo.'*(Al Mughni)*

Na hapa tunazungumzia Manii kama Manii peke yake yalivyo kimaumbile.Kwa maana hio kama ikiwa Manii husika yatakua yamechanganyika na Uchafu wa Najis basi nayo yatakua ni Najis. Kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kwa kututolea Mfano usemao kua: '**Kama tukisema kua Majimaji yanayotoka kwenye Uke wa Mwanamke yatakua sio Tohara basi na Manii yake pia yatakua sio Tohara kutokana na kugusana na Kuchanganyika na Maji maji hayo.Kama vile ilivyokua kwa Mwanamme ambae ataenda Haja Ndogo na Kisha akawa hakunawa kwa Maji kabla ya Kumwaga Manii, basi pia Manii yake Yatakua Najis kutokana na kuchanganyika na Mkojo.'***(Al Majmuu)*

Tunapoangalia kuhusiana na hali hii basi kuna baadi wanaweza wakajiulza masuali kuhusiana na utofauti wa mitizamo pale itakapokua Mtu amelala msikitini na kisha akajimwagia Manii, Jee hukmu yake inakuaje? Hivyo tuangalie mfano huu kulingana na mizamo tofauti ili tufahamiane zaidi.

Kwani katika kujibu Masuali haya basi tutatumia Hadith mbili zinazohusiana na hali mbili tofauti.Ambapo ya kwanza ni ile isemayo kua: **'Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua Nimemuona mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiyapangusa Manii kwenye Nguo yake kwa Mzizi wa Idhkir na alipokua akiyaona yamekauka Nilimuona akiwa anakwangua na kisha Kusalia Nguo hio.**'*(Musnad Imam Ibn Rahawayh)*

Na amesema Imam At Tirmidhii kua: **'Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Manii ni Kama Mafua, hivyo Jipanguseni hata kama kwa Idhkir '***(Imam At Tirmidhi)*

Ambapo amesema Imam Abu Isa Al Tirmdhii kua: **'Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* isemayo kua alikua akikosha Manii kutoka kwenye Nguo za *Rasul AllahSalallahu Alayhi wa Salam,* haipingani na Hadith ya Kupangusa Nguo kutokana nayo na hii ni kwa sababu, hata kama Kupangusa kutatosheleza basi hua inapendekezwa kua Mtu asionekane Mtu akiwa Na amegandwa na Manii.'**

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii katika Fat-Al Barr.Na huo ndio pia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal.Na katika Mtizamo huu basi Ndio tunapata Jibu la Mtizamo wa kwanza kua Kutokana na kua Manii ni Tohara kama tulivyofafanua hapo kabla, basi inaruhusika kwa Mtu Kusali na Nguo yenye Manii, na katika Sehemu iliyomwagikiwa na Manii na Sala inasihi.

Ila sasa tunaona kua Manii pia yamenasibishwa na Mate na Mafua yaani ni kitu ambacho kinakinyaa, na ndio maana ikapendekezwa kua kama ni mabichi basi Yapanguswe na kama yamekauka basi yakwangurwe. Kwani ukiyawacha hua ni sawa na Kusali Na Nguo yenye Mafua, au kusalia sehemu ambayo mtu amepenga Mafua au ametema mate na kisha wewe ukasalia hapo hapo juu yake huku ukiyaona Mate hayo au mafua utajisikiaje? Nafikiri tumefahamiana!

Hivyo baada ya kuangalia Mtizamo huo kulingana na kua Manii ni Tohara.Basi na tuangalie kwa upande mwengine ambao ni ule usemao kua Manii Si Tohara ni Najis ambao ni mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Abu Hanifa.Na kwa upande wao tunatumia hadith nyengine Isemayo kua:

حَدَّثَنَا أَبُو الْيَمَانِ، أَخْبَرَنَا شُعَيْبٌ، عَنِ الزُّهْرِيِّ، ح وَقَالَ اللَّيْثُ حَدَّثَنِي يُونُسُ، عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، أَخْبَرَنِي عُبَيْدُ اللَّهِ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُتْبَةَ، أَنَّ أَبَا هُرَيْرَةَ، أَخْبَرَهُ أَنَّ أَعْرَابِيًّا بَالَ فِي الْمَسْجِدِ، فَثَارَ إِلَيْهِ النَّاسُ لِيَقَعُوا بِهِ فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " دَعُوهُ، وَأَهْرِيقُوا عَلَى بَوْلِهِ ذَنُوبًا مِنْ مَاءٍ ـ أَوْ سَجْلاً مِنْ مَاءٍ ـ فَإِنَّمَا بُعِثْتُمْ مُيَسِّرِينَ، وَلَمْ تُبْعَثُوا مُعَسِّرِينَ

Amesema Abu Al Yaman kua amesema Shuaibu kua amesema Al Zuhriyi kua amesema Al Layth kua amesema Yunus, kua amesema Abu Shihab kua amesema Abdillah Ibn Abdillahi Ibn Utataybah kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: Kuna Bedui alikua akikojoa Msikitini, na hivyo Masahaba wakakimbilia kutaka Kumpiga Lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaamrisha Masahaba kumwachia hadi amalize haja yake kisha akawaamrisha kua Wachukue Maji Ndoo nzima waimwagie katika sehemu iliyokojolewa. **Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Hakika Mmeletwa kwa ajili ya Kurahisisha mambo na wala si kwa ajili yaKuyafanya yawe Magumu.'***(Sahih Bukhari na Muslim)*

Kwa maana hio basi, kutokana na kua Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Abu Hanifa kua Manii ni Najis basi hii inamaanisha kua Sala ya Mtu husika hua ni Batili, kutokana na Najis kwenye Nguo zake na pia kutokana na kua na Najis katika sehemu aliyosalia hadi Nguo hio au Sehemu hio itoharishwe.

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'aala* katika Quran baada ya *Bismi Allahi Rahmani Rahiim:*

﴿بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ۞ يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡمُدَّثِّرُ ۞ قُمۡ فَأَنذِرۡ ۞ وَرَبَّكَ فَكَبِّرۡ ۞ وَثِيَابَكَ فَطَهِّرۡ﴾

Ya Ayyuha Al Muddaththiru; Qum Fa-Andhir; Wa Rabbuka Fakabbir; Wa Thiyabaka Fattahir*(Surat Al Muddaththir 74:1-4)*

Tafsir: ***Ewe Uliejifunika GubigubiNyanyuka Uonye. Na Mola Wako Umkuze kwa KumtukuzaNa Nguo zako Zitoharishe.***

Na amesema pia Asma Bint Abu Bakr *Radhi Allahu Anha* kua: **'Kuna Mwanamke alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: Ya Rasul Allah Jee tufanyeje kama ikiwa Damu ya Hedhi imedondokea kwenye Nguo zetu?.'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua: '**Kama ikiwa Damu ya Hedhi imedondokea kwenye Nguo ya yeyote yule basi na aishike Sehemu hio yenye tone la Damu hio na kisha aisugue na kuikosha kwa Maji, na kisha anasali na nguo hio'***(Sahih Bukhari)*

Hivyo basi kulingana na Mtizamo wa kua Manii no Najis kama zilivyo Najis nyenginezo na kulingana na vithibitisho hivi basi kulingana na Madhhab yote tunaona kua Hukmu yake ni Kua Sala ya Mtu husika itakua ni Batili, kutokana na Nguo na sehemu aliyoisalia kutokua Tohara kwa sababu ya Najis husika.

Ambapo hii inamhusu pia kila atakaejua kua sehemu aliyosalia si Tohara hadi pale sehemu hio itakapotoharishwa, ambapo jambo hili tutafafanua zaidi tukifikia kwenye Najis ya Haja ndogo na Kubwa

na hukmu ya Udhu wa wenye matatizo ya Mikojo. Inshaa Allah. Hivyo hio kama ikiwa Mtu anajua kuhusiana na Najis husika katika sehemu husika.

Lakini kama ikiwa hajui yaani Tuseme aliekojoa mwengine na aliekuja Sali sehemu hio mwengine na hapatatojarishwa na Mtu huyo asiejua amekuja kujua baada ya kusali kua kumbe sehemu ilikua si tohara na yeye ameshamaliza kusali.Basi juu ya hili kulingana na mtizamo wa Abd Allah Ibn Umar, *Radhi Allahu Anhu,* Imam Ataa, Imam Said Ibn Musayyib na kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Malik basi Sala ya Mtu husika hua ni sahih na hatokua na Wajibu wa kuirudia Sala hio.

Lakini kwa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Ahmad basi Sala hio itakua ni Batili na itabidi irudiwe.

Kwa maana hio basi Kama Manii yatakua yameambatana na Uchafu basi nayo yatakua Machafu na hivyo kila sehemu yatakapo mwagikia iwe kwenye Nguo, Mashuka ya Kulalia n.k basi nayo itabidi yatoharishwe kwa Kufuliwa na Maji safi na Sabuni Mara tatu kwa nia ya kuondoa Najis hio.

Hivyo tunafunga Mada ya Utohara wa Manii kwa kukumbushana kua: '**Wanazuoni wanakubaliana kua Manii yakitoka basi humuwajibikia yule yaliemtoka kukoga Janaba.'**

Ambapo anasema tena Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kama ikiwa Mtu atatokwa na Manii na Kisha akakoga Janaba, na kisha akatokwa tena na Manii basi huwajika kukoga tena, iwe Manii hayo yalimtoka baada ya Kukokojoa au Kabla yake.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

GHUSL - KUJITOHARISHA KWA KUKOGA KOGO LA JANABA

❖❖❖❖

Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿يَا أَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ إِذَا قُمْتُمْ إِلَى ٱلصَّلاةِ فٱغْسِلُواْ وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى ٱلْمَرَافِقِ وَٱمْسَحُواْ بِرُؤُوسِكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى ٱلْكَعْبَينِ وَإِن كُنتُمْ جُنُباً فَٱطَّهَّرُواْ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَآءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ ٱلْغَائِطِ أَوْ لاَمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيداً طَيِّباً فَٱمْسَحُواْ بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ مِّنْهُ مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَـٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo idha qumtum ila alssalati faighsiloo wujoohakum waaydiyakum ila almarafiqi waimsahoo biruoosikum waarjulakum ila alkaAAbayni wa-in kuntum junuban faittahharoo wa-in kuntum marda aw AAala safarin aw jaa ahadun minkum mina algha-iti aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban faimsahoo biwujoohikum waaydeekum minhu ma yureedu Allahu liyajAAala AAalaykum min harajin walakin yureedu liyutahhirakum waliyutimma niAAmatahu AAalaykum laAAallakum tashkuroona*(Surat Al Maidah 5:06)***

Tafsir: ***Enyi wale ambao mlioamini! Mnapotaka kufanya Ibada ya Sala, basi kosheni Nyuso zenu na mikono yenu hadi kwenye visugudi, pitisheni mikono yenu (iliyoroa maji) kwenye vichwa vyenu na kosheni miguu yenu hadi juu kwenye viungio vya visigino. Na kama mkiwa mko katika hali ya Janaba, basi jitoharisheni kwa kukoga. Lakini kama mkiwa mnaumwa au mko safarini au mmoja wenu akiwa amejisaidia au ikiwa mmegusana na Mwanamke na hamkupata Maji, basi fanyeni Tayammam kwa kutumia Mchanga msafi na panguseni nyuso zenu na mikono yenu kutokana nao. Allah hataki kukuwekeni katika hali ya kua na ugumu na anataka kukutoharisheni na kukukamilishieni neema zake juu yenu ili mpate kua ni wenye Shukurani.***

Ambapo anasema *Mujaddid Ad Din Mujtahid Imam* Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: *Maenno ya Allah Subhanah wa Taala* yasemayo kua:

وَإِن كُنتُمْ جُنُباً فَٱطَّهَّرُواْ

Wa-in kuntum junuban faittahharoo

Na kama mkiwa mko katika hali ya Janaba, basi jitoharisheni kwa kukoga.

Kilugha yanamaanisha kua ni Kukoga Janaba kutokana na Kuingiliana Kimwili, na hii ni kwa sababu Waarabu wanasema kua kama Mtu akiwa na Janaba yaani hua ni kutokana na kua ameingiliana kimwili, na Wanasema kua hii inamaanisha kua kama Mtu akiwa ameingiliana Kimwili na Mkewe na hii ni kutokana na Hadith na pia kulingana na mtizamo wa Kilugha.

Ambapo Wanazuoni wanakubaliana kua kitendo cha kutokwa na Manii hua kinajulikana pia kama Janaba.Na hii ni kwa sababu amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Kutokana na Manii kuna Kukoga.'** *(Imam At Tirmidhi)*

Na ingawa amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua:

خَرَجْتُ مع رَسولِ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ يَومَ الاثْنَيْنِ إلى قُبَاءَ حتَّى إذَا كُنَّا في بَنِي سَالِمٍ. وقَفَ رَسولُ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ علَى بَابِ عِتْبَانَ فَصَرَخَ به، فَخَرَجَ يَجُرُّ إزَارَهُ، فَقالَ رَسولُ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ: أعْجَلْنَا الرَّجُلَ فَقالَ عِتْبَانُ: يا رَسولَ اللهِ، أرَأَيْتَ الرَّجُلَ يُعْجَلُ عَنِ امْرَأَتِهِ ولَمْ يُمْنِ، مَاذَا عليه؟ قالَ رَسولُ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ: إنَّما المَاءُ مِنَ المَاءِ.

'Nilitoka mimi pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika siku ya Jumatatu kuelekea katika maeneo ya Quba, na tulipokua kwa Banu Salim basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasimama kwenye Mlango wa Itban na kumwita. Itban akaja huku akiwa anaburura Seruni yake.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema 'Tumemharakisha huyu Mtu'**

Itban akasema: 'Ya Rasul Allah! Jee unasemaje kuhusiana na mtu ambae alikua anaharakisha kuingiliana na mkewe lakini akawa hakumaliza kumwaga Manii, jee ni nini hukmu yake?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Wajibu wa Kujimwagia Maji ni Kutokana na Maji.'** *(Sahih Muslim)*

Ambapo hadithi hii inaonesha namna *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyokua akiwafundisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* kuhusiana na umuhimu wa tohara na usafi kwa Waumini na pia

inatuonesha namna Masahaba hao walivyokua na Utiifu na hamu ya kutaka kujua juu ya Hukumu za Dini ya Kiislam katika maisha yao ya kila siku.

Kwani Hadith Inatuonesha kua Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu*alipokua anaelekea katika mji wa Qubah pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*katika Jumatatu moja. Basi walipofika kwenye maeneo waishio watu wa Banu Salim ambao ni wenye kutokana na kabila la Al Khazraj la watu wa Madina, wakaelekea kwenye nyumba ya Itban Ibn Malik Al Ansari *Radhi Allahu Anha* na kisha walipofika nyumbani kwake mlangoni basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwita Itban Ibn Malik Al Ansari *Radhi Allahu Anhu* kwa sauti kubwa. Ambapo hapa inatuonesha kua inaruhusika kwa Mtu kumuita mwenzake kwa sauti kubwa pale anapofika Nyumbani wa mtu husika kutangazia kuwasili kwake.

Na Itban *Radhi Allahu Anhu* aliposikia wito huo basi aliwacha kila kitu alichokua akifanya ikiwemo kumuingilia Mke wake, kwa sababu huo ni wito wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambao hautakiwi kudharauliwa, na akakimbilia kwa haraka sana kwenye wito huo huku akiwa anaiburura Izar yake yaani Nguvo inayovaliwa na Mwanamme Kiunoni kama Kikoi au Seruni.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alipomuona Itban Radhi Allahu Anhu akiwa katika hali hiobasi akawa na wasiwasi kua amemharakisha Itban kutokana na aliyokua akiyafanya na hivyo akamwambia Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua: **‘Tumemharakisha huyu Itban kuachana na aliyokua akiyafanya’**

Hivyo Itban *Radhi Allahu Anhu* alipofika kwa *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* akamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: **‘Ya Rasul Allah jee unaonaje kuhusiana na mtu ambae alikua akiharakisha kuachana na kuingiliana na mke wake kabla hajamwaga Manii? Inambidi akoge Janaba ama la?’**

Na *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* akasema: ‘**Wajibu wa Kujimwagia Maji ni Kutokana na Maji.**’ Yaani Kukoga Janaba hua kunawajibishika pale itakapokua Mtu amemwaga Manii, na hivyo basi kama ikiwa Mtu hakumwaga Manii basi huya hana Wajibu wa kukoga Janaba mbali ya kua amemuingilia Mke wake.

Ambapo hii ndio iliyokua Hukmu ya mwanzo kuhusiana na Jambo hili katika kipindi cha mwanzoni mwa Miaka ya Uislam, lakini hata hivyo Hukmu hii ilikuja kubatilishika pale aliposema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* baadae katika Hadith za Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua:

أَنَّ النَّبِيَّ صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ قال: «إذا جَلَس بيْنَ شُعَبِها الأَربعِ، ثمَّ جَهَدَها، فقدْ وجَبَ الغُسلُ»،

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ‘Kama Mwanamme akikaa baina ya viungo Vinne vya Mwili vya Mwanamke na kisha akaikandamiza juu yake (Kwa Kumuingilia) basi hua kuna Wajibu wa Kukoga Janaba.*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo kwenye Hadith ya Imam Muslim basi kuna maneno yasemayo kua

وإنْ لم يُنزِلْ فوُجوبُ الغُسلِ

‘Hata kama hakumwaga Manii basi huwajibika kukoga Janaba’

Hivyo basi Wajibu wa kukoga Janaba hua ni wa Kila Mtu ambae amemwaga Manii, na pia kila atakaeingiliana na mwenza wake iwe katika kuingiliana huko wamemwaga Manii ama la.

Na amesema Imam An Nawawi kua:

وَلَوْ أَنْزَلَتْ الْمَرْأَةُ الْمَنِيَّ إلَى فَرْجِهَا فَإِنْ كَانَتْ بِكْرًا لَمْ يَلْزَمْهَا الْغُسْلُ حَتَّى يَخْرُجَ مِنْ فَرْجِهَا لِأَنَّ دَاخِلَ فَرْجِهَا فِي حُكْمِ الْبَاطِنِ وَلِهَذَا لَا يَلْزَمُهَا تَطْهِيرُهُ فِي الِاسْتِنْجَاءِ وَالْغُسْلِ فَأَشْبَهَ إحْلِيلَ الذَّكَرِ وَإِنْ كَانَتْ ثَيِّبًا لَزِمَهَا الْغُسْلُ لِأَنَّهُ يَلْزَمُهَا تَطْهِيرُ دَاخِلِ فَرْجِهَا فِي الِاسْتِنْجَاءِ فَأَشْبَهَ الْعُضْوَ الظَّاهِرَ

Kama ikiwa Manii ya Mwanamke yatafikia kwenye Uke wake, basi Mwanamke huyo kama akiwa ni Bikira ambae hajaolewa au hajawahi kuingiliwa kimwili basi hua hana Wajibu wa kukoga Janaba hadi pale Manii hayo yatakapotoka nje na kumwagika kutoka kwenye Uke wake, kwa sababu sehemu ya ndani ya uke wake hua inahesabika kua ni sehemu ya ndani ya mwili wake. Hivyo hua haina haja kwake kujisafishe ndani ya uke wake, wala kukoga Janaba kwani hukmu yake hua ni sawa na hukmu ya Uume.

Lakini kama Mwanammke huyo akiwa ni Thayyib yaani alieolewa au aliekwishawahi kuingiliwa hapo kabla basi hua ni Wajibu kwake kukoga Janaba kwa sababu hua ni Wajibu kwake kujisafisha ndani ya Uke wake katika wakati wa kufanya kujitoharisha Uke (Istinja) na hivyo hukmu yake hua ni ile ya sehemu inayoonekana ya mwili wake. *(Al-Majmu' Sharh al-Muhadhdhab*)

Ambapo kwa upande wa Imam Al Khattab Al Maliki, Al Habib Imam Hasan Ibn Ahmad al-Kaff na Imam Al Khatib Al Shirbini wameelezea kuhusiana juu ya hili kwa kusema kua: **'Kwa Mwanamke ambae ni Bikira basi hua ni Wajibu kwake kukoga Janaba mara baada ya Manii kua ni yenye kutoka nje ya Uke wake. Ambapo kwa upande wa Mwanamke ambae ni Thayyib basi hua ni Wajibu kwake kukoga Janaba pale inapokua Manii yametoka na kufikia katika sehemu ya ndani ya Uke ambayo hua ni wajibu kwake kuikosha pale anapofanya Istinja, ambayo ni sehemu inayokua inaonekana pale Mwanamke anapokua amechutama au anapojisaidia haja ndogo, hata kama Manii hayo yatakua hayajatoka nje kabisa ya uke wake'**(*Al Mughni al-Muhtaj, Al Mausu'ah Al Fiqhiyyah Al Kuwaitiyyah, Mawahib Al Jalil fi Syarh Mukhtasar Khali)*

Na kwa upande mwengine pia baadhi ya Wanazuoni wanasema kua: **'Kama ikiwa Mwanamke anaenda kufanya uchuguzi kwa Daktari ambae atamtia vidole kwenye Uchi wake, na Mwanamke huyo akapata hisia za Matamanio basi Mwanamke huyo huwajibikiwa kukoga Janaba.'**

Ila amesema Imam Ali Al Shurunbulali Al Hanafi kua: **'Kama ikiwa Mume ataingiza Kidole kwenye moja kati ya sehemu mbili za Siri za Mkewe, hua hakuwajibishi kukoga Janaba.'***(Nur Al Idah Maa Maraqi Al Falah)*

Ama kuhusiana na namna ya kukoga Janaba basi kuna Hadithi tofauti zinazoelezea juu yake kama vile:

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ يُوسُفَ، قَالَ أَخْبَرَنَا مَالِكٌ، عَنْ هِشَامٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ عَائِشَةَ، زَوْجِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم كَانَ إِذَا اغْتَسَلَ مِنَ الْجَنَابَةِ بَدَأَ فَغَسَلَ يَدَيْهِ، ثُمَّ يَتَوَضَّأُ كَمَا

يَتَوَضَّأُ لِلصَّلاَةِ، ثُمَّ يُدْخِلُ أَصَابِعَهُ فِي الْمَاءِ، فَيُخَلِّلُ بِهَا أُصُولَ شَعَرِهِ ثُمَّ يَصُبُّ عَلَى رَأْسِهِ ثَلاَثَ غُرَفٍ بِيَدَيْهِ، ثُمَّ يُفِيضُ الْمَاءَ عَلَى جِلْدِهِ كُلِّهِ.

Amesema Abd Allah Ibn Yusuf kua amesema Malik, kua amesema Hisham kua amaesema Baba yake kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua:'Wakati *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipokua anataka kukoga Janaba Alikua akianza kwa kukosha Mikono yake kisha Hutia Udhu kama anaetaka kusali na kisha Hutia Vidole vyake Maji na Kuvipitisha kwenye Mizizi ya Nywele zake, na kisha hujimwagia Magao Matatu ya Maji Kichwani mwake, na kisha Hujimwagia Maji Mwili mzima.'*(Sahih Bukhari)***

Ambapo amesema Al Qadhi Abu Shujaa Al Shafii kua:

والذي يوجب الغسل ستة أشياء: ثلاثة تشترك فيها الرجال والنساء وهي التقاء الختانين وإنزال المني والموت وثلاثة تختص بها النساء وهي الحيض والنفاس والولادة

Yanayojumuisha Kujitoharisha kwa Kukoga ni mambo 6, Matatu kati yao yanamhusu Mwanamme na Mwanamke ambayo ni:

1-Zinapokutana Sehemu za Siri za Mwanamme na kuingia ndani ya sehemu za Siri za Mwanamke.

2-Kutokwa na Manii kwa Mwanamme au Mwanammke.

3-Kufariki.

Na yaliyobakia Matatu yanamhusu Mwanammke peke yake ambayo ni: Hedhi, Nifasi na Kujifungua*(Ghayat Al Taqrib)*

Kisha Imam Abu Shujaa anaendelea kusema kua: '**Maimamu Wanne (Nuuman Ibn Thabit Abu Hanifa, Malik Ibn Anas, Muhammad Idris Al Shafii na Ahmad Ibn Hanbal) wanakubaliana juu ya Mambo Manne kati ya haya kua ndio yenye kuhitajia Kukoga Janaba ambayo ni:Kukutana kwa kuingiliana kwa Mbili za Siri za Mwanamme na Mwanamke, Kutoa Manii, Hedhi na Nifas.'**

Na wanasema Wanazuoni kua kama mtu atakua amelala katika kitanda kimoja na mweziwe ambae anaweza kumwaga Manii pia, na kisha walipoamka wakaona Manii, na ikawa hawajui ni nani miongoni mwao aliejimwagia Manii hayo. basi hukmu yake kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ni kua Inapendekezwa kua kila mmoja miongoni mwao akoge Janaba. Mbali ya kua hakuna ulazima.

Ambao kaupande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: 'Kukoga Janaba hua nilazima kwa wote wawili.'

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: 'Kama Watu hao itakua ni mtu na mkewe, basi Wajibu wa kukoga Janaba huya ni wa Mume tu na hii ni kwa sababu Manii huya ni yenye kumwagwa na Mwanamme, na kama ikwa hawakuoana na Kukoga Janaba huya ni Wajibu kwa wote wawili.

Ambapo hakuna utofauti kuhusiana na Watu waliooana na wasiooana kihukmu katika Madhhab Mengine.

Na tunapozungumzia kuhusiana na Kukoga Janaba basi wenye Lugha yao hutumia neno Ghusl badala ya Kukoga Janaba.Na Imam Abu Shujaa anaendelea kutuambia kuhusiana na Ghusl au Kukoga Janaba kua: '**Kama alivyosema An Nawawi kua Neno Ghusl ikiwa likiwa litatamkwa na Fat-ha basi hua linamaanisha Kuufunika Mwili kwa Maji, na hivyo basi hua haihitajiki Kuusugua Mwili husika kama Walivyosema Wafuasi wa Imama Malik Lakini kama ikiwa neno Ghusl Lilatatamkwa Dhamma basi hua linamaanisha Kuukosha Mwili kwa Maji. Kwa mfano kama Ikiwa Mtu ikiwa ataingia katikati ya Bahari Na kufunikwa na Maji kwa nia ya Kujitojarisha, basi Mtu huyo ataruhusika Kusali baada yake, na hii ni kwa sababu ya kua ametoharika iwe kama aliingia Kichwa chini Miguu Juu au Kichwa Juu.**

Kwa sababu unapokosha sehemu ya Mwili basi hua unakosha Mwili mzima kutokana na kua wote ni Mwili mmoja Na Mpangilio hua hauna Umuhimu sana katika Kukoga Janaba. Hivyo Ghusl au Kukoga Janaba hua ni Kuukosha Mwili kwa Maji bila ya Ulazima wa Kuusugua, na Ushahidi Juu ya hili ni kulingana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua.

رأى رجلاً يجلس في مؤخرة المسجد فقال النبي صلى الله عليه وسلم: لم لم تصل؟ قال: يا رسول الله! أصبحت جنباً ولا ماء) فعلمه النبي صلى الله عليه وسلم أن يتيمم, وأنه يكفيه عن الماء؛ لأن التيمم فرع عن أصل، (ثم أتي النبي صلى الله عليه وسلم بذنوب أو بدلو من الماء فقال: قم فأفرغه على جسمك) ولم يشترط الدلك.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuona Mtu akiwa amekaa Nyuma kabisa Msikitini, na hivyo akamuuliza: 'Kwanini wewe Hukusali?'**

Mtu huto akasema: 'Ya Rasul Allah hakika Mimi siko Tohara Na hakuna Maji.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamfundisha Mtu huyo Kutayammam, jambo ambalo lilimtosheleza Mtu huyo kua Tohara bila ya kutumia Maji.Na kisha mara yakaletwa Maji kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Mtu huyo.

'Sasa Nyanyuka na Ujimwagie Maji haya kwenye Mwili wako' na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumwambia Mtu huyo kua ajisugue.

Na pia aidhan

وأيضاً لما سألته أم سلمة رضي الله عنها عن اغتسال المرأة (أفتنقض ضفائرها؟ قال: لا, إنما يكفيك أن تحثي ثلاث حثيات على رأسك, ثم أفيضي الماء على جسدك، بذلك تكونين قد طهرت

Ummu Salama*Radhi Allahu Anha* aliulizwa kuhusiana na Ghusl ya Mwanamke ambapo nae kua jee afumue Nywele? Nae akasema: La Sio Lazima kwani itatosheleza kwako wewe Kujimwagia Magao Matatu ya Maji Kichwani na kisha Kujimwagia maji Mwilini mwako na Utakua Tohara.

Hivyo Kauli hizi za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* zinaonesha kua Kujisugua hua si Lazima kwa Mtu mwenye Kukoga Janaba.' *(Ghayat Al Taqrib)*

Ambapo kwa upande mwengine basi anasema Maymuna *Radhi Allahu Anha* kua: '**Mimi nilimpelekea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Maji kwa ajili ya Kukoga Janaba.Nae akakosha Mikono yake mara 3 na kisha akachota Maji kwa Mkono wake wa Kulia na Kujimiminia katika sehemu za Siri huku akizikosha kwa mkono wa kushoto**. **Na kisha akaupangusa Mkono huo wa kushoto ardhini kwa nguvu na kisha akatia Udhu kama wa Sala.**

Kisha akajimwagia Magao Matatu ya Maji.Kichwani na kisha akamalizia kuukosha Mwili mzima, na kisha akaondoka katika Sehemu aliyokogea na kukosha Miguu yake. Nami nikampa Taula lakini hakuichukua.'*(Sahih Muslim)*

Ambapo amesema Imam An Nawawi kuhusiana ha Hadith hii kua: **'Hadith hii inamaanisha kua inapendekezwa kwa mtu atakaefanya Istinjaa kwa Maji, basi atakapomaliza kukosha mikono yake kwa mchanga au mti (kama Mharita unaotengenezewa Sabuni) au ausugue na mchanga au na ukuta wa dogo ili kuondoa uchafu kutokana nao'***(Sharh Sahih Muslim)*

Na kasema Imam Al Kharshi Al Maliki kua: **'Inapendekezwa kukosha mikono baada ya istinjaa kwa mchanga, udongo au vitu kama hivyo kwa ajili ya kuondoa harufu ya uchafu.'***(Mukhtasar Al Khalil)*

Na Imam Al Bukhari ana ahadith isemayo kua '**Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua:**

أنَّ امْرَأَةً سَأَلَتِ النبيَّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ عن غُسْلِهَا مِنَ المحِيضِ، فأمَرَهَا كيفَ تَغْتَسِلُ، قالَ: خُذِي فِرْصَةً مِن مَسْكٍ، فَتَطَهَّرِي بهَا قالَتْ: كيفَ أتَطَهَّرُ؟ قالَ: تَطَهَّرِي بهَا، قالَتْ: كيفَ؟ قالَ: سُبْحَانَ اللَّهِ، تَطَهَّرِي فَاجْتَبَذْتُهَا إلَيَّ، فَقُلتُ: تَتَبَّعِي بهَا أثَرَ الدَّمِ

Kuna Mwanamke alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Tohara ya baada ya kumaliza siku zake za Hedhi. Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamfahamisha namna yakukoga na kisha akamwambia; 'Chukua kipande cha pamba chenye Miski na Kisha Jitoharishe kutokananacho' Mwanamke huyo akauliza: 'Nijitoharishe Vipi?' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia : 'Jitoharishe kutokana nacho' Mwanamke huyo akauliza : 'Vipi?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia : 'Subhanah Allah, Jitoharishe kutokana nacho.'**

Aisha *Radhi Allahu Anha*anasema kua: 'Hivyo mimi nikakichukua kipande Cha pamba chenye Miski na kumwambia: Kichukue kisha jipake kufuatisha sehemu zilizoathirika kwa Damu.'*(Sahih Bukhari)*

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Daud yeye amenukuu hadith hii ikiwa an maneno yasemayo:

قالَتْ كيفَ أتطهَّرُ بها قال سبحانَ اللهِ تَطهري بها واستَتِري بثوبٍ وزادَ وسألَتْهُ عنِ الغسلِ منَ الجنابةِ ، فقال : تأخُذينَ ماءَكِ فتطهرينَ أحسنَ الطُّهورِ وأبلغَهُ ثم تَصُبِّينَ على رأسِكِ الماءَ ثم تدلُكينَهُ حتى يبلغَ شؤونَ رأسِكِ ثم تُفيضينَ عليكِ الماءَ قال وقالَتْ عائشةُ نِعمَ النساءُ نساءُ الأنصارِ لم يكنْ يَمنعُهنَّ الحياءُ أن يسألْنَ عنِ الدينِ وأن يتفقَّهنَ فيه

Mwanamke huyo akauliza : 'Nijitoharishe Vipi?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia: 'Subhanah Allah, Jitoharishe kutokana nacho na kisha jifunike na nguo.'**

Mwanamke huyo akamuuliza*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kuhusiana na kujitoharisha kutokana na Janaba. *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia : 'Chukua maji yako, kisha jitoharishe nayo vizuri sana kwa kadiri utakavyoweza. Kisha jimwagie kichwani na ujisugue hadi uhakikishe kua kila mzizi wa nywele zako kua umeroa. Kisha jimwagie Maji mwili mzima.'

Hivyo Aisha *Radhi Allahu Anha*akasema kua: '**Wanastahiki Pongezi Wanawake wa Kiansari kwa sababu Hisia za Haya hazikuwazuia wao kuuliza masuali kwa kina katika kutaka kuifahamu Dini ya Kiislam.**'*(Imam Abu Daud)*

Na amesema *Abu Hurayra Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* kua:

كُلِّ شَعَرَةٍ جَنَابَةٌ، فَاغْسِلُوا الشَّعَرَ، وَأَنْقُوا الْبَشَرَةَ

'Chini ya Kila Unywele kunahitajika Kogo la Janaba hivyo zikoshe Nywele na isugue Ngozi'*(Sunna At Tirmidhi, Sunan Abu Daud, Sunan Ibn Majah)*

Na ingawa kila sehemu ya Ngozi ya Mtu Hua inatakiwa kua ipate kuguswa na Maji, lakini hata hivyo kama ikiwa kuna Mtu ambae kazi zake ni zenye kuhusiana Gundi au Rangi na hivyo baadhi ya sehemu ya ngozi zake, kwa mfano kwenye vidole labda ikawa imeganda kama Super Glue kwa mfano na hivyo kua ni ngumu kuitoa basi hii hua ni dharurah ambayo hua haina tatizo na hivyo haina haja ya kuanza kujikwangua kwa sababu ya kutaka kuitoa Super Glue hio kwenye Ngozi au Rangi husika mpaka ukajisababishia Madhara, kwani katika hali kama hii basi hua inaruhusikana hivyo Udhu au Kogo la Janaba hua linasihi.

Hivyo hizi ni baadhi tu ya Hadith za Ghusl ambazo tukiziangalia zote kwa Ujumla basi tunaona kua Ghusl au Kukoga Janaba kunajumuisha hatua zifuatazo:

1-Kutia Nia ya Kujitoharisha kwa Kukoga kutokana na Uchafu(wa Janaba au Hedhi, au Nifas).

2-Kusema Bismi Allahi Rahmani Rahiim na kisha Kuosha Mikono mara 3 na kisha kukosha sehemu za Siri.

3-Kutia Udhu kama wa Sala.

4-Kujimwagia Maji Kichwani mara 3 hadi Ngozi yote ya Kichwa iroe maji.

5-Kukosha Upande wa Kulia wa Mwili mara 3, kisha upande wa Kushoto mara 3 na kisha kujimwagia Maji mwili mzima kwa kuhakikisha kua kila sehemu ya ngozi yako imeingia Maji yaani Imekua katika hali ya Ghusl.

6-Inapendekezwa Kutumia sabuni na kujisugua ili kusafika zaidi.

Na ingawa Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Nia ya kukoga Janaba, lakini wengi wao miongoni mwao wanakubaliana kua Nia kwa ajili ya kukoga Janaba hua ni wajibu na hii ni kulingana na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal kama ilivyoelezewa katika.*(Mukhtasar Khalil, Mughni al-Muhtaj - Imam al-Khatib al-Sharbini na Kashshaf al-Qina' cha Imam al-Bahuti).*

Na hii ni kwa sababu Nia ya kukoga Janaba hua ni Wajibu kwa sababu Kukoga kwenyewe kwa ajili ya kujitoharisha hua ni sehemu ya Ibada, na Ibada hua na ulazima wa kua na nia juu yake, na hii ni kulingana na Hadith ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndani yake kua:

إِنَّمَا الأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ

‘Hakika ya Amali hua ni kulingana na Nia’

Na Imam Al Khatib Al Shirbini amesema kua: **‘Ni Muhimu kujua kua Sehemu ya Nia hua ni ndani ya Moyo wa Mtu husika**’*(Al Iqna)*

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anasema kua: **‘Mtizamo unaotegemewa zaidi katika Madhhab yetu ya Imam Al Shafii ni Kua Nia hua ni Sunnah inayopendekezwa.**’*(Minhaj Talibin)*

Ambapo amesema Qadhi Abu Bakr Ibn Al Arabi Al Maliki kua: **‘Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na Udhu katika wakati wa Kukoga Janaba kua Sehemu ya Kukoga Janaba na Nia ya Kujitoharisha kwa kukoga Janaba hua inachukua nafasi ya Nia ya kujitoharisha kutokana na uchafu.**’

Lakini kwa upande wa Imam Al Haskafi basi yeye anasema kua: **‘Kulingana na mtizamo wa Madhhab yetu ya Hanafi Nia ya kukoga Janaba hua ni Sunna na wala si Wajibu’***(Durr Al Mukhtar)*

Hivyo anasema Imam Firazbadi Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii katika kitabu chake cha Al Muhadhdhab fi Fiqh Al Imam Al Shafii kua: **‘Muainisho wa Nia hua ni kunuia kujitoharisha kutokana na uchafu wa Najis, au kujitoharisha kwa kujitoa Najis husika. Na Nia yeyote ile mtu atakayonuia hua inatosheleza kulingana na kusudio lake mtu husika ambalo ni kujitoharisha kutokana na Najis hio.’(***Al Muhadhdhab fi Fiqh Al Imam Al Shafii***)**

Kwa mfano unaweza kusema:

اللهم إني نويت هذا الغسل لرفع الحدث الأصغر والأكبر والجنابة والتطهر من المذي أو الودي أو المني والبول، والطهارة عامة.

Ya Allah nanuia kogo hili kwa kujitoharisha Najis Ndogo na Najis kubwa, na Janaba na Kujitoharisha na Madhii, Madii na Mkojo na kujitoharisha na kwa kila kitu kiujumla.

Hivyo hua inaruhusika kuchanganya nia kwa mfano kwa upande wa Wanawake ambae atakua ameingiliana na Mume wake na kisha akalala bila ya kukoga na baada ya kuamka asubuhi akajikuta kua ameingia kwenye Siku zake, hivyo katika hali kama hii Mwanamke hua anaruhusika kujitoharisha kwa Kujumuisha Nia ya kukoga Janaba pamoja na Hedhi kama anavyosema Imam Ahmad Ibn Naqib Al Misri kua: **'Mwanamke anaehitajia kujitoharisha kutokana na Janaba na kujitoharisha kutokana na Hedhi anaweza kwa kujitoharisha kwa Nia ya kukoga aidha kati ya moja ya haya kwani hua inatosheleza kwa yote.'***(Umdat Al Salik)*

Na akasema Shaykh ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: **'Wanasema Wanazuoni wetu kua: Inapendekezwa kwa mtu kunuia ndani ya Moyo wake na pia kutamkwa kwa ulimi wake kama vile ilivyo kwenye Sunnah za Udhu, hivyo kama mtu akithibitisha kwenye Moyo wake bila ya kutamka basi hua inatosheleza na kama mtu akitamka neno la Kukoga Janaba lakini ndaniya Moyo wake ikawa kuna mtizamo mwengine basi hua kinahesabiwa kile kilichomo Moyoni mwake.**

Na kama mtu akinuia kukoga bila ya kusema kujitoharisha kutokana na Janaba, basi hua haitoshelezi na hii ni kutokana na mtizamo unaokubalika zaidi. Hivyo kama ikiwa kuna Mwanamke amekoga kwa ajili ya Hedhi kwa ajili ya kumruhusu Mume wake kumuingilia, basi hua kuna mitizamo tofauti juu yake.

Ambapo Mtizamo ulikokua sahih ni kua kila kinachoruhusika baada yake kama kuingiliana, kusali kufunga n.k hua kinaruhusika.

Mtizamo wa pili ni kua hakuna hata kimoja kinachoruhusika. Na Mtizamo wa Tatu ni kua Ni Kuingiliana tu ndiko kunakoruhusika.

Hivyo kama Mtu ikiwa atatia nia ya Kutia Udhu kwa ajili ya kUsali na kisha ikawa hakusali basi Udhuu wake huo hua ni batili, na hii ni kutokana na kupingana kwa nia yake nakitendo chake.

Lakini kama Mtu ikiwa atalazimika kujitupa ndani ya Mto na kishandaniyake anuie kukoga Janaba basi kukoga kwake huko hua ni kwenye kukubalika.

Na kama ikiwa mtu atajitoharisha viungo vyote vya mwili wake isipokua miguu yake na kisha akatumbukia kwenye Mto na hivyo miguu hio ikaroa maji huku mtu huyo akiwa kwenye nia yake basi Tohara yake itakua Sahih, na Ibada ya Sala yake itakua Sahih, kwani vyenginevyo basi miguu yake itakua haikutoharika, nah ii ni kulingana na mtizamo unaokubalika zaidi.

Na kama mtu akiingia kwenye kisimamo cha Sala kwa nia ya Sala na kisha akatokea mtu anemdai na akamlipa basi Sala yake itakua sahih. Na imetajwa katika Al Shamil kua: Kama mtu atanuia kutoka kwenye udhu baada ya kumaliza kutia Udhu basi Udhu wake hua haujakatika na hii ni kulingana na Mtizamo unaokubalika zaidi.'*(Rawdha Talibin wa Umdat al Muftin)*

Na anasema Imam Muhammad Ibn Kasim Al Ghazi Al Shafii kua: 'Kama ikiwa Mtu hatotia Udhu lakini Kogo lake la Janaba limemrowesha Mwili Mzima, basi Imam Ibn Abd Al Barr na wengineo wamesema kua: **'Mtu huyo atakua ametekeleza Wajibu wa kukoga Janaba kwa sababu amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua**

﴿وَإِن كُنتُمْ جُنُباً فَٱطَّهَّرُواْ﴾

Wa-in kuntum junuban faittahharoo *(Surat Al Maidah 5:06)*

Tafsir: ***Na kama mkiwa mko katika hali ya Janaba, basi jitoharisheni kwa kukoga.***

Na kuna Makubaliano ya Wanazuoni bila ya kupingana juu ya hili.''*(Sharh Rawdha)*

Na kama ikiwa Mtu atanuia kutia Udhu na kukoga Janaba, na kisha akavunja Udhuu wake, basi hua anaruhusika Kumalizia Kukoga Janaba na kisha akatia Udhu.

Ambapo kwa upande wa Imam Al Kharashi: '**Kama ikiwa Mtu atajitharisha huku akijiwekea mpaka wa Kujitoharisha kukoga Janaba bila ya kutia Udhu basi hii itamtosheleza, na hii ni kwa ajili ya kukoga Janaba tu, lakini hua haichukui nafasi ya Udhu, kwani Udhu hua ni wenye kutakikana kwa kila Mtu anaesali'***(Mukhtasari Al Khalil)*

Na Imam Abu Bakr Ibn Al Arabi akasema kua: '**Wanazuoni hawakutofautiana kuhusiana na Udhu ndani ya Kukoga Janaba na kua Nia ya kujitoharisha kutokana na Janaba hua inaitangulia ni ya Udhu na kuchukua nafasi ya Udhu kwa sababu yanayojumuisha Tohara ya Janaba ni mengi zaidi kuliko yanayojumuisha Tohara ya Udhu, hivyo yale yaliyokua kidogo hua yanajumuishwa na Nia ya yale yaliyo mengi, na hivyo Nia hutosheleza kwa vyote.'**

Ama kuhusiana na Suali la Kukoga Janaba kabla ya kulala au baada ya kuamka ambalo mara kwa mara watu hua wanaulizana ambalo inabidi tuliangalie kwa sababu Suali hilo pia waliulizana *Masahaba Radhi Allahu Anhum* kama inavyoelezewa katika Hadith ifuatayo:

Amesema Qutaybah Ibn Said kua amesema Layth kua amesema Muawwiyyah Ibn Salih kua amesema Abd Allah Ibn Abi Qays*Radhi Allahu Anhu*kua:

سَأَلْتُ عَائِشَةَ عن وِتْرِ رَسولِ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ فَذَكَرَ الحَدِيثَ، قُلتُ: كيفَ كانَ يَصْنَعُ في الجَنَابَةِ؟ أكانَ يَغْتَسِلُ قَبْلَ أنْ يَنَامَ؟ أمْ يَنَامُ قَبْلَ أنْ يَغْتَسِلَ؟ قالَتْ: كُلُّ ذلكَ قدْ كانَ يَفْعَلُ، رُبَّما اغْتَسَلَ فَنَامَ، ورُبَّما تَوَضَّأَ فَنَامَ.

Mimi nilimuuliza *Ummu ul Muuminina* Aisha *Radhi Allahu Anha*kuhusiana na Witr ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* ambapo nae akanitajia Hadith.

Kisha mimi nikamuuliza: 'Jee *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifanya nini anapokua na Janaba? alikua akikoga kwanza kabla ya kulala au akikoga baada ya kuamka?'

***Ummu Ul Muuminin* Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema: 'Alikua akifanya yote hayo, kwani baadhi ya wakati alikua akikoga Janaba kwanza kabla ya Kulala na baadhi ya wakati alikua akitawadha na kisha analala.'**

Abd Allah Ibn Qays anaendelea kusema kua: 'Mimi nikasema Shukran zote anastahiki *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambae amerahisisha kila kitu.'*(Sunan An Nasai, Sahih Ibn Khuzaymah, Imam At Tirmidhi)*

Naam hii ni miongoni mwa Hadith ambazo zinazungumzia kuhusiana na Tohara ya Mwili mzima wa Ibn Adam. Ambayo kuhitajika kwake hua ni kutokana na mabadiliko ya Kimaumbile ya Mwili na Ufahamu wa Ibn Adam baada ya kumalizika Vitendo vya Kutokwa na Manii, Hedhi na Nifasi.

Ambavyo hua ni vyenye kumpelekea Ibn Adam kutokua na Utohara wa Kumuabudu Mola wake, hadi pale atakapojitoharisha kwa Kukoga Janaba. Na kwa Kua Dini ya Kiislam ni Dini yenye kusimamia Mfumo wa Maisha aliyouamriaha Muumba yaani *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaejua kila kitu juu ya Viumbe wake basi ametutumia Muongozo usiokua na Ugumu ndani yake kupitia kwa Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na vitendo vya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ndio Muongozo unaostahiki kufuatwa, ambapo mmoja kati ya Miongozo hio basi ni kuhusiana na Janaba ambao ndani yake unatuonesha kua inaruhusika baada ya Kua na Janaba kulala kabla ya kukoga na pia kukoga kabla ya kulala na hii ni kulingana na wepesi wa hali ya Mtu aliyokua nayo katika wakati husika.

Na juu ya hili pia kuna hadith isemayo kua;

حَدَّثَنَا سُفْيَانُ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ دِينَارٍ، عَنِ ابْنِ عُمَرَ، عَنْ عُمَرَ، أَنَّهُ سَأَلَ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَيَنَامُ أَحَدُنَا وَهُوَ جُنُبٌ قَالَ يَتَوَضَّأُ وَيَنَامُ إِنْ شَاءَ وَقَالَ سُفْيَانُ مَرَّةً لِيَتَوَضَّأْ وَلْيَنَمْ

Amesema Sufyan kua amesema Abd Allahi Ibn Dinar kua amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* ambae alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema:

Ya Rasul Allah Jee inaruhusika kwa Mtu kulala wakati akiwa na Janaba?

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Naam, na anaweza kutia Udhu na kisha akalala kama atataka.**'*(Musnad Imam Ahmad)*

Na amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Ingawa inaruhusika kutokoga Janaba hadi katika Wakati wa Sala ya Al Fajir, lakini inapendekezwa Kutia Udhu kabla ya Kulala, na Kuna Makubaliano ya Wanazuoni juu ya Hili.' *(****Al Majmuu)***

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali katika Al Mughni. Na kama tunakumbuka basi tuliwahi kuzungumzia Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua:

حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، قَالَ حَدَّثَنَا يَحْيَى، قَالَ حَدَّثَنَا حُمَيْدٌ، قَالَ حَدَّثَنَا بَكْرٌ، عَنْ أَبِي رَافِعٍ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم لَقِيَهُ فِي بَعْضِ طَرِيقِ الْمَدِينَةِ وَهْوَ جُنُبٌ، فَانْخَنَسْتُ مِنْهُ، فَذَهَبَ

فَاغْتَسَلَ، ثُمَّ جَاءَ فَقَالَ " أَيْنَ كُنْتَ يَا أَبَا هُرَيْرَةَ ". قَالَ كُنْتُ جُنُبًا، فَكَرِهْتُ أَنْ أُجَالِسَكَ وَأَنَا عَلَى غَيْرِ طَهَارَةٍ. فَقَالَ " سُبْحَانَ اللَّهِ، إِنَّ الْمُؤْمِنَ لاَ يَنْجُسُ "

Amesema Aliyu Ibn Abd Allahi kua amesema Yahya kua amesema Humayd kua amesema Bakru kua amesema Abi Rafii kuaAbu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikutana na mimi katika Moja kati ya Mitaa ya Madina huku mimi nikiwa na Janaba.**

Hivyo nikamchomoka na kuenda kukoga na kisha nikarudi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na nilipofika basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Ewe Abu Hurayrah Ulikua wapi?'

Hivyo nami nikajibu kwa kusema *Ya Rasul Allah* Mimi nilikua na Janaba hivyo sikupenda kukaa pamoja nawe.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema:'*Subhanah Allah!* Muumini kamwe hawezi kua Najis.**'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo Mujaddid Ad Din Al Hafidh Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii anasema kuhusiana na Hadith hii kua: **'Hadith hii inatuonesha kua kwa Mtu ambae ana Janaba na anatakiwa ajitoharishe basi anaruhusika kucheleweshe Kukoga Janaba na akafannya shughuli zake nyenginezo kwanza kisha ndio akakoga.'** *(Fat-h Al Barr)*

Ambapo Imam An Nawawi amesema pia kua: '**Inapendekezwa kwa Mtu kusafisha sehemu zake za Siri, na kutia Udhu kabla ya kufanya mambo yake mengineyo, hususan kama ikiwa mtu anataka kumuingilia mke wake wa pili ambae hajamuingilia.Na As-hab Al Wujuh wetu wamesema kua haipendekezwi Kulala, Kula, Kunywa, au kuingiliana tena bila ya kutia Udhu na Hadith zinathibitisha hivyo. Hivyo hakuna kutokukubaliana kwenye Madhhab yetu juu ya kua Udhu si Lazima na huu pia ndio Mtizamo wa Malik na wengi miongoni mwa Wanazuoni.**'*(Sharh Sahih Muslim)*

Na tukirudi tena katika Hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Suali la *Umar Ibn Al Khattab Radhi Allahu Anhu* alilomuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na kukoga basi tnaona kua ingawa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na wengineo wanasema kua Udhu Sio Lazima lakini wapo Wanazuoni wasemao kua ni Wajibu kutia Udhu.

Hivyo anasema Shaykh Ul Islami Al Hafidh Taqi Ad Din Abu Fat-h Muhammad Ibn Ali Ibn Daqaiq Al Idd Al Shafii kuhusiana na Hadith hii kua: **'Hadith hii iko katika hali ya Kufananisha na pia katika Hali ya Kushurutisha na hivyo kuwaunga Mkono wale Ambao wanawajibisha kutia Udhu kabla ya kulala wakati ukiwa na Janaba. Kama vile alivyosema Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Barr Al Maliki kua: Ingawa Wengi miongoni mwa Wanazuoni ni wenye kusema kua Inapendekezwa kutia Udhu, lakini pia kuna wanaopinga Mtizamo huo na kusema kua Udhu hua ni Wajib, Jambo ambalo si la kawaida.'**

Ambapo Imam Ibn Abi Shaybah amenukuu hadith isemayo kua: **'Amesema Shaddad Ibn Aws kua Kama ikiwa Mmoja wenu atakua na Janaba katika wakati wa Usiku na kisha akataka Kulala. Basi na Atie Udhu kwa sababu Udhu hua ni Nusu ya Kukoga Janaba.'**

Na Imam Ibn Daqaid Al Idd basi anasema kua: 'Amesema Al Shafii kuhusiana na Jambo hili kua halimhusu Mwanamke mwenye Hedhi, na hii ni kwa sababu hata kama akitia Udhu basi Najisi yake hua haiondoki jambo ambalo ni tofauti na mwenye Janaba. Lakini hata hivyo kama Damu yake itasita kutoka, basi hua inapendekezwa kwake kutia Udhu. Kwani katika Hadith imethibitishwa kua Kutia Udhu kwa ajili ya kujitoharisha na Janaba hua haina ulazima wa hapo hapo, bali imewekewa Mpaka wa kua hadi pale Mtu atakapotaka kuenda kusali,hivyo inapendekeza kujitoharisha kabla ya kulala.

Imam Ibn Jawzi yeye amesema kua: 'Hikma iliyomo ndani pendekezo la Kutia Udhu ni kua Malaika hukaa mbali ya Mtu mwenye Janaba, mwenye Najis, mwenye Harufu mbaya, n.k jambo ambalo hua ni kinyume chake kwa upande wa Shaytan.'(Fat-Al Barr Imam Ibn Hajar Al Asqallani)

Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Ali Ibn Umar Ibn Muhammad Al Tamimi Al Mazari al Maliki basi yeye anasema kua: **'Wacha Mtu alale akiwa katika hali ya moja kati ya Tohara mbili hizi(aidha akoge Janaba au atie Udhu) kutokana na Khofu ya Kua huenda akafariki wakati akiwa usingizini.'**

Naam..hivyo basi kuhusiana na Jambo hili tunaona kua kama Mtu ukiwa na Janaba hua ni Bora kukoga kabla ya Kulala, kama huwezi basi tia Udhu na kama huwezi pia basi japo kukosha sehemu zako za Siri kisha lala, na kama haiwezekani hata hivyo basi hua hamna kosa lolote juu yako. Kwani hata kama ukitoka Jasho basi Mwili na Jasho la Mtu mwenye Janaba hua si Najis.

Naingawa kukoga Janaba hua ni Wajib kulingana na hali tulizozitaja lakini pia kuna hali ambazo huya ni Sunna inayopendekezwa kukoga Janaba, kwani Wanazuoni wamependekeza pia kwa kusemakuani Muhimu kuianza Siku ya Sikukuu kwa Kukoga kama unavyokoga Janaba kabla hujatoka Nyumbani kwako Asubuhi, hata kama hukuamka na Janaba kwani kufanya hivyo hua ni miongoni mwa Sunna za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*

Na pia ndivyo Walivyokua wakifanya Masahaba *Radhi Allahu Anhum* akiwemo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Salamah Ibn Aqwa *Radhi Allahu Anhu* n.k ambako hua kunaashiria Utahara kamilifu wa Kimwili na Kinafsi. Hivyo hata kama huna Janaba basi hua inapendekezwa kua katika Asubuhi ya Siku ya Idd Kukoga Janaba kabla ya Kutoka kama vile ambavyo inavyopendekezwa katika kila Siku ya Ijumaa.

Kwani amesema **Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallau Alayhi wa Salam* kua:**

إِذَا جَاءَ أَحَدُكُمُ الجُمُعَةَ، فَلْيَغْتَسِلْ.

'Inapomfikia mmoja wenu Siku Ya Ijumaa basi na Akoge Janaba.'*(Sahih Bukhri na Muslim)*

Ambapo hii ni hadithi iliyonukuliwa na Imam Nafii ambae nae amenukuliwa na Maimamu zaidi ya mia tatu juu ya hadithi hii, na mbali ya hadithi hii ikunuuliwa na Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* lakini pia hadithi hii imenukuliwa na Masahaba zaidi ya 24.

Na hivyo kuna baadhi ya Wanazuoni kutokana na Usahih wake Hadith hii basi wameichukulia Hukumu iliyomo ndani yake kua ni Wajibu kukoga Janaba katika siku ya Ijumaa, kama alivyosema Imam An Nawawi kua: **'Wajibu wa kukoga Janaba umenukuliwa na baadhi ya Wanazuoni wa Kizazi cha Mwanzoni cha Uislam.'** Ambapo Mtizamo huyu pia ndio mtizamo wa Imam Ibn Al Mundhiri Al

Nishapuri ambae yeye ameinukuu hadithi hii kupitia kwa Abu Hurayrah, *Radhi Allahu Anhu,* Ammar ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* na Malik Ibn Anas *Radhi Allahu Anhu.*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Kattabi basi yeye amenukuu Mtizamo huu kua pia ni wa Imam Hasan Al Basr, na Imam Ibn Hazim ameunukuu kutoka kwa Masahaba kadhaa wa *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam,* na Tabiina na Tabii Tabiina.

Kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Ibn Sharaf An Nawawi kua**: 'Uthibitisho unaochukuliwa kua ni Ushahidi juu ya kupendekezwa Kukoga Janaba katika Siku ya Idd ni wa Hadith ya Ibn Umar kulingana na Siku ya Ijumaa.'***(Al Majmuu)*

Ambapo amesema Imam Sulayman Ibn Khalaf Al Baji Al Maliki kua:'**Inapendekezwa Kukoga Janaba kabla ya kutoka kuelekea katika Sala ya Idd, ambapo Imam Ibn Habib amesema kua Wakati Mzuri wa Kukoga Janaba Ni baada ya Kusali Salat Al Fajr, ambapo Imam Malik amesema kua hata baada ya Salat Al Idd pia inakubalik**a.'*(Al Muntaqah Sharh Muwwata)*

Na akasema Muwaffaqah Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua**: 'Kulingana na Mtizamo wa Imam Al Khiraq basi wakati mzuri wa kukoga Janaba katika Siku ya Idd ni baada ya Alfajir**. **Ambapo Imam Al Amidi amesema kua Kukoga Janaba kabla ya Salat Al Fajr hua hakutimizi Sunnah yake,kwa sababu Sunnah ya kukoga hua inatakiwa itekelezwe ndani ya Siku ya Idd na hivyo kabla ya Salat Al Fajr hua haitoshelezi kama vile inavyokua katika siku ya Ijumaa.**

Na Imam Ibn Aqil amesema kua: Kilichotajwa katika Vitabu vya Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na Kukoga Janaba katika Siku ya Idd ni kua unaweza kukoka kabla ya Al Fajr na baada ya Alfajr.

Ambapo Imam Al Amidi amesema kua Kukoga Janaba kabla ya Salat Al Fajr hua hakutimizi Sunnah yake, kwa sababu Sunnah ya kukoga hua inatakiwa itekelezwe ndani ya Siku ya Idd na hivyo kabla ya Salat Al Fajr hua haitoshelezi kama vile inavyokua katika siku ya Ijumaa.

Na Imam Ibn Aqil amesema kua: Kilichotajwa katika Vitabu vya Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na Kukoga Janaba katika Siku ya Idd ni kua unaweza kukoga kabla ya Al Fajr na baada ya Al Fajr Na hii ni kwa sababu Mda wa Salat Al Idd ni Mfupi tofauti na Ijumaa, hivyo ikiwa mipaka yake ni baada ya Salat Al Fajr basi kuna wale ambao watakaoshindwa utekelezwaji wake.

Na kwa kua lengo ni Kukitoharisha basi inakubalika pia kukoga kabla ya Alfajr karibu na wakati wa Sala ya Alfajr, hivyo ni bora kukoga kabla ya Alfajr,ili kujitoa katika Mvutano wa Wanazuoni juu ya hukmu yake.'*(Al Mughni)*

Ambapo anasema Al Qadhi Abu Tayyib Al Tabari Al Shafii kua: '**Amesema Al Shafii kama alivyosema Al Buwayti kua: Ni Sahih Kukoga Janaba katika Siku ya Idd kabla ya Kuchomoza Ju**a.'*(Al Mujarrad)*

Na akasema Imam An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Wakati wa kukoga Janaba katika Siku ya Idd basi kuna Mtizamo Miwili Juu yake. Ambapo Mtizamo Sahih zaid ni kukoga kabla ya Kuchomoza Jua ambao ndio Mtizamo unaokubalika zaid kama ilivyosemaa katika Al Umm, na Mtizamo unaokubalika zaidi miongoni mwa Wanazuoni ni kua aidha kabla au baada ya Salat Al Fajr.**

Ambapo kwa Mtizamo wa Madhhab yetu basi ni kua kama ikiwa tutasema kua Mtizamo sahih ni kabla ya kuchomoza Jua, basi Mtizamo utakaokubalika pia utakua ni katikati ya Usiku, lakini kabla ya hapo yaani ya Nusu ya Usiku hua haikubaliki.

Na Mtizamo wa pili ni kua Inakubalika kukoga katika wakati wowote ule wa Usiku, ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Al Ghazali na ndio Mtizamo unaokubaliwa zaidi na Imam Ibn Al Sabbagh na wengineo. **Na mtizamo wa tatu ni kua inakubalika kukoga kabla ya kuanza Salat Al Fajr, na huu ni Mtizamo wa Imam Al Baghawi**'*(Al Majmuu)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MADHII.

❖❖❖❖

Hivyo ingawa Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Hali ya Manii, kwani kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi kua : '**Manii hua si Najis'**. Na kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua '**Manii Ni Najis'.**

Lakini hata hivyo Wanazuoni wanakubaliana Kuhusiana na Madhii kua ni Najis kama anavyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua Madhii Hua Ni Najis.'***(Sharh Al Muhadhdhab)*

Na pia kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua Madhii hua ni Tofauti Na Manii Kihukmu na hivyo hayamuwajibishi Kukoga yule yaliyomtoka.Kama alivyosema tena Shaykh Ul Islami Imam Abh Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua yule atakaetokwa na Madhii, hua hawajibiki Kujitoharisha kwa Kukoga.Ila kulingana na wengi miongoni mwa Wanazuoni basi ni wenye Mtizamo wa kua Madhii hua yanabatilisha Udhu na hivyo Humuwajibisha Kutia Udhu upya yule yaliemtoka.'***(Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo amesema Al Muhaqqiq Imam Ibn Aabidin Ash Shami Al Hanafi kua: '**Madhii hua ni Maji mepesi yanayoteleza ambayo humtoka Mtu aliekua na Mwamko na hamu ya Kuingiliana Kimwili, ambayo hua ni Najis na hivyo yanapotoka nje ya mwili humpelekea Mtu husika kua ni mwenye kubatilikiwa na Udhu wake.'*(****Radd Al Mukhtar)***

Na amedema Muwafaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Ibn Al Mundhir amesema kua Wanazuoni wanakubaliana kua Kutokwa na Haja Ndogo, Kubwa, Madhii na kutokwa na Gesi hua ni kwenye Kubatilisha Tohara ya Mtu husika hivyo kama Mtu alikua na Udhu basi itambidi atie Udhu tena Upya kutokana navy**o.'*(Al Mughni)*

Na akasema Imam Ad Dardir Al Maliki kua: '**Miongoni mwa Vitu ambavyo ni Najis basi ni Manii, Madhii na Wadii, hata kama ni yenye kua ya Wanyama walioruhusika Kuliwa, kwa vitu vitatu hivyo kutokana na Maumbile yake vitu hivyo na kukirihisha kwake na kuweza kugeukia katika hali ya Uharam na pia kutokana na kua asili yake ni Damu na hivyo kuhalakika kwa uasili wake haumaanishi kuhalalika kwake vitu hivyo.'***(Al Sharh Al Kabir)*

Na amesema Imam Al Shawkani Al Hanbali kua: **'Wanazuoni wakakubaliana kua Madhii Ni Najis'***(Nail Al Awtar)*

Hivyo ingawa Wanazuoni wanakubaliana juu ya kua kua Madhii ni Najis, Lakini pia kwa upande mwengine basi anasema Imam Abd Rahman Ibn Ahmad Ibn Rajab Al Hanbali kua:'**Kuna kauli moja kutoka kwa Imam Ahmad Ibn Hanbal inayosema kua Madhii ni tohara kama yalivyo Manii, ambapo huu ni mtizamo wa Imam Abu Hafs Al Barmaki ambae mmoja kati ya Wanazuoni wetu, na hivyo ametoa Fatwa kua mtu hua anawajibu wa Kujimwagia Maji baada ya kutokwa nayo, na kufanya hivyo hua ni sawa na Ibada.**'*(Fah Al Barr Li Ibn Rajab)*

Na akasema pia Imam Al Mardawi Al Hanbali kua: '**Kuna uthibitisho kutoka kwake Imam Al Barmaki kuhusiana na Utohara wake, ambapo Imam Abu Al Khattab amefuata mtizamo huu pia ktika Al Intisar na Ibn Razin amefafanua juu yake**'*(Al Insaaf)*

Ambapo kuhusiana na nini Madhii basi anasema Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii kua: **'Madhii ni maji mepesi yasiyotoka kwa wingi kama manii, lakni hutoka tone kwa tone katika hali ya matamanio**'.*(Al Hawwi Al Kabir)*

NaImam Abu Maali Al Haramain Al Shafii anasema: **'Madhii ni maji mepesi yasitoka kwa nguvu na hayafuatiwi na hali ya uchovu'**.*(Nihayat Al-Matlab)*

Imam Abu *Al* Husein Yahya *Al* Imrani Al Yamani Al Shafii basi yeye amesema kua: **'Madhi hua ni Najis kutokana na ukweli wa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuamrisha Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*kua akoshe sehemu zake za Siri, na pia Madi ni Najiskwa sababu yako sawa na Madhii.'***(Al Bayyan fi Madhhab Al Shafii)*

Ambapo Imam Ibn Salah amesema kua '**Madhii hua na rangi nyeupe na mazito katika kipindi cha wakati wa baridi hua na rangi ya njanonjano na mepesi katika wakati wa kiangazi.'**

Na Imam Al Amash Amesema kua amesema Imam Mujahid Ibn Sulayman kua: **'Ama kuhusiana na Manii, Madhii na Wadii, basi Manii yanawajibisha Kukoga Janaba lakini Madhii na Madii huya yanawajibisha Udhu.'**

Na Imam Ibn Abd Al Barr Al Maliki Al Andalus amesema kua: **'Ama kuhusiana Madhii ambayo ni yenye kujlikana sana kua ni yenye kutoka pale mtu anapokua anachezeana na Mke wake kwa sababu ya Matamanio anayoyapata kutokana nae, au kwa sababu ya kutoingiliana kwa mda mrefu na Mwanamke, ambapo hii ndio maana ya Suali la msingi la hadith ya Ali Ibn Abi Talib*Radhi Allahu Anhu*ambapo kunamakubaliano ya Wanazuoni juu yake kuhusiana na kuhitajika kwa udhukutokana nayo na hitajio la kuisafisha kutokana nayo ni kwa sababu ya kua Unajis wake'***(Mawsuah Ahami Toharat)*

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii anayaelezea kwa kusema kua: '**Madhii hua ni Maji Mepesi meupe yenye utelezi, ambayo yanapotolewa ndani ya mwili wa Ibn Adam wakati Mtu anapokua na hali ya hisia za Matamanio, lakini bila ya kuhisi raha au starehe katika wakati wa kutoka kwake, na hua hayafuatiwi na hali ya uchovu baada ya kutoka kwake.**

Madhii yanapotoka hua hakuna hisia ya kua sasa hivi ndio yanatoka Ingawa Madhii hua yanawatoka Wanaume na Wanawake, lakini hua yanawatoka Wanawake zaidi.'*(Al Majmuu)*

Imam Abu Bakr Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abi Shaybah anaelezea kuhusiana na Madhii katika kitabu chake cha Musanaf Ibn Abi Shaybah kwa kuainisha hadith zisemazo kua:

حدثنا ابن علية عن سليمان التيمي عن أبي عثمان النهدي أن سليمان بن ربيعة تزوج امرأة من بني عقيل فرآها فلاعبها قال فخرج منه ما يخرج من الرجل قال سليمان أو قال المذي قال فاغتسلت ثم أتيت عمر فقال ليس عليك في ذلك غسل ذلك أيسر

Ibn Ulayyah amesema kua amesema Sulayman Al-Taymi kwa mamlaka ya Abu Uthman Al-Nahdi kwamba Sulayman Ibn Rabi'ah kua alioa Mwanamke kutoka katika kabila la Banu Uqayl. Alikua nae na akachezeana nae. Akasema, "Kisha kitokacho kwa mtu kikamtoka. Sulayman akasema, "Au alisema, 'Madhii''.Akasema, Hivyo nikakoga Janaba, kisha nikamjia Umar na kumwambia ambapo nae akasema, 'Si lazima kukoga Janaba kwa hilo.'

Lakini pia Imam Abu Bakr Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abi Shaybah katika kitabu chake cha Musanaf Ibn Abi Shaybah kua:

حدثنا أبو بكر قال حدثنا هشيم عن زيد بن أبي زياد قال حدثني عبد الرحمن بن أبي ليلى عن علي قال سئل النبي صلى الله عليه وسلم عن المذي فقال فيه الوضوء وفي المني الغسل .

'**Amesema Abu Bakr kua amesema Hisham kua amesema Zayd Ibn Abi Zayd kua amesema Abd Rahman Ibn Abi Layla kua amesema AliIbn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa kuhusiana na Madhii ambapo nae akasema Yanapotoka basi Udhu hua unawajibika, na yanapotoka Manii basi Kukoga Janaba hua kunawajibika.'**

حدثنا هشيم عن منصور عن الحسن عن علي قال كنت أجد مذيا فأمرت المقداد أن يسأل النبي صلى الله عليه وسلم عن ذلك ؛ لأن ابنته عندي فاستحييت أن أسأله فقال إن كل فحل يمذي فإذا كان المني ففيه الغسل وإذا كان المذي ففيه الوضوء .

Na amesema Hisham kua amesema Mansur kua amesema Al Hasan kua amesema Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mimi nilikua nikitokwa sana na Madhii, hivyo nikamuomba Miqdad aniulizie kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana nayo kwa sababu Binti yake *(Fatima Bint Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam)* ndie Mke wangu, hivyo nilikua nnaona haya kumuuliza.**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Kila Mwanamme hua ni mwenye kutokwa na Madhii, hivyo kama mtu atatokwa na Manii basi itambidi kukoga Janaba, lakini kama yakimtoka Madhii basi na Atie Udhu tu.'

حدثنا محمد عن بشر قال حدثنا مسعر عن مصعب بن شيبة عن أبي حبيب بن يعلى بن منية عن ابن عباس أنه أتى أبيا ومعه عمر فخرج عليهما فقال إني وجدت مذيا فغسلت ذكري وتوضأت فقال عمر أو يجزئ ذلك ؟ قال : نعم ، قال : سمعته من النبي صلى الله عليه وسلم ؟ قال : نعم .

Na amesema Muhammad kua amesema Bishr kua amesema Musar kua amesema Musar Ibn Shaybah kua amesema Abu Habib Ibn Yalah Ibn MunyahKua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: Nilienda kwa Abu Bakr na Umar *Radhi Allahu Anhum* na nikawaambia:Hakika mimi nimejikuta nna Madhii hivyo nikaukosha Uume wangu na kisha Nikatia Udhu.

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akauliza kwa kusema: Jee hivyo hua inatosheleza?

Nami nikasema: 'Naam!'

Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* akasema : 'Jee umemsikia wewe *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m akisema hivyo?'.

Nami Nikasema : 'Naam.'

حدثنا أبو معاوية عن الأعمش عن سليمان بن مسهر عن خرشة بن الحر قال سئل عثمان عن المذي فقال ذاك القطر ومنه الوضوء

Na amesema Abu Muawwiyah kua: '**Amesema Al Amash kua amesema Sulayman Ibn Musahir kua amesema Kharshah Ibn Al Har kua:Uthmani Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* aliulizwa kuhusiana na Madhii ambapo nae akasema: Hua Ni Matone yanayotoka na hivyo Udhu hua unatosheleza juu yake.'**

حدثنا ابن علية عن خالد عن أبي قلابة عن عمه أبي المهلب قال كان من أهله إنسان يغتسل من المذي يخرج بعد البول فقال له أما إن الوضوء يجزي عنه .

Na amesema Ibn Ulayyah kua amesema Khalidkua amesema Abu Qilabah kua amesema Ami yake ambae ni Abu Al Muhallab kua: '**Mmoja kati ya watu wa miongoni mwa Familia yangu alikua akikoga Janaba kwa sababu ya kutokwa na Madhii baada ya kumaliza haja ndogo hivyo nikamwambia kua Kwa Madhii basi Udhu tu hua unatosha.'**

حدثنا وكيع عن عكرمة بن عمار عن عبد ربه بن موسى عن أمه عن عائشة قالت المني منه الغسل والمذي والودي يتوضأ منهما

Na amesema Imam Wakii kua: '**Amesema Iqrimah Ibn Ammar kua amesema Abd Rahman Ibn Musa kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: 'Manii yanawajibisha Kukoga Janaba lakini Madhii hua yanawajibisha Udhu.''**

حدثنا المحاربي عن ليث عن مجاهد عن أبي هريرة أنه سئل عن المذي فقال ذاك النشاط فيه الوضوء

Na akasema Al Maharibi kua: '**Amesema Al Layth kua Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* aliulizwa kuhusiana na kutokwa na Madhii, ambapo nae akasema: Hilo ni Jambo linalowajibisha kutia Udhu.**

حدثنا أبو الأحوص عن سماك قال قلت للحسن البصري أرأيت الرجل إذا أمذى كيف يصنع فقال كل فحل يمذي فإذا كان ذلك فليغسل ذكره .

Na amesema Abu Al Hawas kua amesema Samak kua: **'Nilimuuliza mimi Hasan Al Basr kuhusiana na Madhii ambapo nae akasema: 'Kila Mwanamme hua anatokwa na Madhii hivyo ikitokea hivyo basi wacha ajisafishe kwa kukosha Uume wake.''**

حدثنا ابن فضيل عن الأعمش عن مجاهد قال المني والودي والمذي ففي المني الغسل والودي والمذي الوضوء

Ibn Fadil alituambia kutoka kwa Al-A'mash kwa mamlaka ya Mujahid, ambaye alisema: Manii, maji ya shahawa, na maji ya kabla ya kumwaga shahawa yanahitaji wudhuu wa kiibada. Shahawa zinahitaji kuoshwa kiibada, wakati maji ya shahawa na maji ya kabla ya kumwagwa kwa shahawa yanahitaji wudhuu.

Naam hivyo ni baadhi ya vithibitisho vilivyomo katika Kitabu cha Musanaf Ibn Abi Shaybah kuhusiana na Madhii na hivyo kuthibitisha kua Madhii yanapotoka hua yanatengua Udhu na hivyo humpelekea yule yaliemtoka akajisafishe kwanza na kisha atie udhu upya.

Na Amesema Sahl Ibn Hunayf kua:

كنتُ ألقَى مِنَ المذْيِ شدةً وعناءً ، فكنتُ أُكْثِرُ منه الغسلَ . فذكرْتُ ذلِكَ لِرَسولِ اللهِ صلَّى اللهُ - عليْهِ وسلَّمَ وسألتُهُ عنْهُ ؟ فقال : إِنَّما يجزِئُكَ منْ ذلِكَ الوضوءُ فقلتُ يا رسولَ اللهِ ، كيْفَ بما يُصِيبُ ثوبِي منْهُ ؟ قال : يكفيكَ أنْ تأخُذَ كفًّا مِنْ ماءٍ فتنضَحَ بِهِ ثوبَكَ حيثُ ترَى أنَّهُ أصابَ مِنْهُ

Mimi nilikua ni Mtu ambae nna matatizo ya Kutokwa na Madhii sana, na hivyo ilikua kila wakati nnakoga Janaba. Hivyo nikamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana nayo ambapo nae akaniambia kua Udhu tu hua unatosheleza kwa Madhii. Hivyo nami nikamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: Jee vipo kuhusiana na yataingia kwenye Nguo zangu?

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Itakutosheleza kama utachukua gao la Maji na kumwagia kwenye sehemu ya nguo yako ambayo unadhania kua imeingia Madhii.'(Sunnan Abu Daud, Sunan At Tirmidhii, Sunnah Ibn Majah, Sunan Ad Darimi Musnad Imam Ahmad)*

Na katika Musnad Ahmad Ibn Hanbal kuna Hadith ya Ali Ibn Abi Talib Radhi Allahu Anhu ambayo ina maneno tofauti kidogo na Hadith aliyoinukuu Imam Ibn Abi Shaybah ambayo tulinukuu jana, kwani hii inasema:

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ سَعِيدٍ، عَنْ هِشَامٍ، أَخْبَرَنِي أَبِي أَنَّ عَلِيًّا، رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ لِلْمِقْدَادِ سَلْ رَسُولَ اللَّهِيَغْسِلُ ﷺعَنْ الرَّجُلِ يَدْنُو مِنْ الْمَرْأَةِ فَيُمْذِي فَإِنِّي أَسْتَحْيِي مِنْهُ لِأَنَّ ابْنَتَهُ عِنْدِي فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ ذَكَرَهُ وَأُنْثَيَيْهِ وَيَتَوَضَّأُ.

Amesema Yahya Ibn Said kua Hisham kua amesema Baba yake kua Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* alimtuma Miqdad akamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Mwanamme ambae akimkaribia Mwanammke tu basi hua anatokwa na Madhii.

Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* akaendelea kusema kua: Kwa sababu mimi naona haya kuuliza kwani Binti yake ndio Nimemuoa mimi. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Mwache Mtu kama huyo akoshe Uume wake na Korodani zake na Kisha Atie Udhu.'*(Musna Imam Ahmad)*

Naam..nimeinukuu hadithi hizi mbili kwa sababu Wanazuoni ndio hua wanazitumia sana hadith hizi kama vigezo katika Kutoa Hukmu juu ya Madhii na kujitoharisha kwake kimwili na kimavazi.Ambapo kuhusiana na Madhii yanapotoka katika Mwili basi kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal na pia mtizamo wa Imam Al Awzai hua wanasema kua:**'Inatakiwa kukosha viungo vyote vilivyotajwa yaani Uume na Korodani pia, na hii ni kwa sababu viungo hivyo vimetajwa.'**

Ambapo Mtizamo wa Wanazuoni waliobakia basi wao wanasema kua: '**Ni Wajibu kukosha sehemu ya kiungo tu cha mwili iliuoguswa na Madhii hayo.'**

Na kuhusiana na Nguo basi ingawa Imam Muhammad Idris Al Shafii na Imam Is-haq Ibn Rahawayh wanasema kua: Kuikosha Nguo husika hua ni Wajibu, na hii ni kukingana na kauli ya sehemu ya hadith iliyoshurutisha Kukosha.

Lakini kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab mengineyo basi wao wanasema kua, kilichoshurutishwa kukoshwa katika hadith ni Sehemu za Siri tu na wala sio nguo.

Hivyo ingawa wengi kati ya Wanazuoni wanasema kua inatosheleza kumwagia maji katika sehemu ya nguo iliyoingia Madhii kama ilivyotajwa katika Hadith ya Sahl Ibn Hunayf, ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema Inatosheleza kumwagia gao la maji katika sehemu iliyoingia Madhii.Na pia kwa kua Madhii ni Najis basi hua yanatengua Udhu na hivyo mtu akitokwa nayo basi anatakiwa ajisafishe Uume wake na Korodani zake na kumwagia Maji kwenye sehemu ya Nguo iliyomwagikiwa itatosheleza.'*(Masail Fi Sharh Muslim Imam An Nawawo, Fat-Al Barr Imam Ibn Hajar Al Asqallani, Subulan Salam na Nail al awtar)*

Na tunyaporudi kwenye hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* aliemtuma Miqdad kumuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Mwanamme ambae akimkaribia Mwanammke tu basi hua anatokwa na MadhiiKwa sababu yeyeanaona haya kuuliza kwani

amemuoa Binti yake. Na ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akasema:Mwache Mtu kama huyo akoshe Uume wake na Korodani zake na Kisha Atie Udhu.**

Basi anasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kuhusiana na hadith hii kua: **Hii ni hadith ambayo Mnyororo wa nukuu yake hauuliziki masuali kutokana na usahih wake, hivyo Madhii hua ni Najis na Uume na Korodani pia inabidi zikoshwe baada ya kutoka kwake, kutokana na kua hua kunabatilisha Usafi wa Kiibad*a****(Al Talkhis)***

Na Nimeirudia hadithi hii kwa sababu huenda watu wakajiuliza ni kwa nini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akashurutisha na Korodani pia zitiwe maji kukoshwa?

Ambapo ili kupata lake suali hili basi haina haja kutafuta vitabu vya Elimu ya Sayansi ya Biolojia bali tunarudi kwenye vitabu vyetu sisi kwa Wanazuoni wetu ambao mmoja wao aitwae Imam Muhammad Shams Ul Haq Aadhimabdi Al Hanafi anatuambia kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema hivi Kwa sababu Korodani zinapotiwa Maji ya baridi basi Maji ya baridi hayo hua ni yenye Kuyakimbiza, au kuyarudisha Madhii Ndani*** *(Awn Al Maa'bud)*

Naam..hio ndio Hikma ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, Mtume ambae hajui kusoma wala hajui kuandika lakini hapo hapo ni mwenye kusema yale ambayo yanawashangaza hata wenye kujua kusoma.Na hii ni kwa sababu moja kati ya sifa kuu za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni kua:

﴿وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ﴾

Wama Yantiqu Aani Al Hawa - Na Wala Hasemi kutokana na Matamanio Yake

﴿إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ﴾

In Huwa Illa Wahyun Yuuha - (Maneno yake) Hua si chochote isipokua Ni Wahyi Aalioshuyshiwa.***(Surat An Najm 53:3-4)***

Naam kwa kua Madhii hua Ni Najis basi hua inabidi yaondolewe Athari zake kwenye kitu husika kama zinavyoondolewa Najis.Ambapo imesemwa kwenye Bushra Al Karim na Nail Al Rajaa kua:

Najis ziko za aina tatu:

1-Najasa Al Mughalladha -Najis Nzito kama zitokanazo na Mbwa au Nguruwe.

2-Najasa Al Mukhaffafa - Najis Zilizokua Hafifu kama Mkojo wa Mtoto mdodo asiezidi miaka miwili.

3-Najasa Al Mutawassita - Najis za Kati na kati kama Madhii, Madii, Pombe, Mkojo n.k.

Na katika kusafisha Naji basi hua ni kulingana na kilichomo ndani ya Najis husika ambazo hua za aina mbili ambazo ni:

Kuna Najasa Ainiyyah yaani Najis ambayo Inaonekana kwa rangi au hali, inasikikana kwa Harufu au Ladha.

Na kuna Najasa Hukmiyah yaani Najis ambayo haionekani kutokana na kua haina hali wala harufu wala rangi wala ladha.

Hivyo kukosha Najasa Ainiyyah basi kwanza inatakiwa Kukisafisha kitu husika kwa kukiondoa Athari zote za Najis hio husika.

Yaani Kitu kisafishwe hadi muonekano wa Najis hio au Harufu au Ladha au Rangi itoweke na kisha unamalizia kwa kumwagia Maji safi kitu husika. **Hivyo Kama athari ya Harufu au rangi au Ladha itabakia basi itabidi usafiahe tena kwa kutumia sabuni ili kuondoa athari husika ukisha maliza utamwagia Maji kuondoa Sabuni na kukikamua kiru husika au kukikunuya na kisha utamwagia maji tena na kukunuta au kukamua na kuanika kama utataka.*(Bushra Al Karim na Nail Al Rajaa)***

Ama kuhusiana na Najasa Al Hukmiyya basi kwa kua haionekani wala haina harufu wala rangi wala ladha basi utamwagia Maji tu kitu hicho ili kuondoa Athari hio na kukunuta au kukamua na kwa kua ni Najis isiyoonekana basi hata mara moja tu hua inatosha**.** Hivyo Mtu utatoharisha kitu kulingana na hali ya Najis husika kama tulivyoelezea.

Na kama Najis huysika imemwagkia katika kitu kama Sakafu, Ukuta, Marumaru, na vitu vyenginevyo basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kama Najis ikiwa imemwagikia kwenye Kitu kigumu, kama Kisu, Upanga, Kioo (MaruMaru) n.k, basi hua haiwezekani kusafisha kwa kuipangusa Bali vinatakiwa Visafishwe kwa Kukoshwa kama vikoshwvyo vitu vyenginevyo, ambapo huu pia ni Mtizamo wa Ahmad na Daud**. **Lakini kwa mtizamo wa Malik na Abu Hanifa basi wao wanasema kua vitu hivyo vinaweza kuafishwa kwa kupangusw**a.'(*Al Majmuu)*

Kwani amesema Imam Al Kasani Al Hanafi kua: '**Kama Najis ikiingia kwenye Kitu ambacho ni Kigumu na Kilichonyooka kama Upanga, Kioo n.k basi hua inaweza kuondolewa kwa kukikwaruza kitu hicho iwe kwa kutiwa maji Au bila ya kutiwa Maji, na hii ni kwa sababu Najis hio hua haiwezi kuzama ndani ya kitu hicho, hivyo kitu hicho kinaweza kusafishwa kwa kupanguswa au kukwaruzw**a.'*(Badai Al Sanai)*

Na akasema Imam Ad Dasuqi Al Maliki kua: '**Kama ikitokezea kua Najis imwangukia kwenye kitu kigumu ambacho itakua na khofu kua kama kikitiwa maji basi kitaharibika kwa mfano kama upanga n.k**. **Basi tutachukulia kiasi ya kulinganisha na kukubalika kwa Damu,yaani hata kama ikiwa ni nyingi basi haitotiliwa maanani, na hii ni kutokana na khofu ya kukiharibu kitu husika.'** *(Hashiya Al Dasuqi Ala Sharh Al Kabir)*

Hivyo ni kama ikiwa kitu hicho hakitomeza Najis hio ndani yake lakini kama ikiwa kitu hicho kitameza Najis hio ndani yake kwa mfano kama sehemu ya Ardhi.Ambapo anasema Imam An Nawawi juu ya hili kua **'Kinachotakiwa katika kuondoa Najis katika sehemu ambayo imezama ndani yake kama kwenye Ardhi basi hua ni kumwagia Maji mengi sana kiasi ya kua Sehemu hio itaimeza au itainyonya Najis hio ndani yake**. **Na kuna baadhi wasemao kua inatakiwa sehemu husika kumwagiwa Maji mara saba, ambapo mtizamo huu sio sahih.**'*(Al Majmuu)*

Na amesema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua: '**Kuna watu wasemao kua inatakiwa Maji yamwagwe kwa Idadi kadhaa, yaani kwa makisio Ya Najis ya Mbwa, na kuna wasemao kua haina haja ya kuhesabu mara ngapi, bali muhimu ni kumwaga maji mengi juu ya Najis husika hadi Najis itoweke, na huu ni Mtizamo wa Imam Al Shafi**i.'*(Al Mughni)*

Ama kuhusiana na pale inapokua Mtu ametokwa na Madhii lakini yuko katika Mazingira ambayo hakuna Maji jee afanyeje?

Naam imeandikwa kwenye *Mawsuah Al Fiqhiyyah* kua: **'Madhii ni Najis, na kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ni kua Kutokana nayo Basi Mtu anatakiwa ajitoharishe kwa Maji au kwa Kijiwe.**

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik ambao ni tofauti na Mtizamo unaokubalika na wengi miongoni mwa Wanazuoni wao.Na huu ndio Mtizamo unaokubalika zaidi kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, ila kwa upande wa Madhhab ya Imam Hanbal mtizamo huu unakubalika kutokana kunukuliwa mara moja.

Kwani kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Ahmad Ibn Hanbal basi ni kua Kutumia Maji ni Lazima, na hivyo kutumia Vijiwe, n.k hua haisihi, na hii ni kwa sababu ya Hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* aliyosema kua Mimi nilikua nikitokwa sana na Madhii na nikajisikia Aibu kumuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya hilo kwa sababu nimemuoa Binti yake.

Hivyo nikamtuma Miqdad Al Aswad ambae akaniulizia na akaambiwa kua, Mtu kama huyo mwache akoshe uume wake na korodani zake na kisha atie Udhu. Na katika Hadith nyengine amesema kua Wacha akoshe Uume wake na kisha atie Udhu.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi Kukoga hua ni lazima kama itakua Madhii yametokana na kupatikana hisia za raha, lakini kama ikiwa hakuna hisia hizo basi mtu anaweza kutumia vijiwe,pale itakpokua sio jambo linalotokea kila siku kama tatizo la mkojo kwani ikiwa linatokea kula siku basi itakua ni dharurah inayomruhusu kutotilia maanani.'*(Mawsuah Fiqhiyyah)*

Ambapo kujisafisha huko hua kunajulikana kama Al Istinjaa yaani Njia ya Kujisafisha Najis kwa kuanzia kwenye sehemu iliyotoka Najis husika.

Na amesema Imam Ibn Abd Al Barr kua: **'Amrisho la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na kujisafisha sehemu za Siri kutokana na Madhii kwa kutumia maji kukosha kitu chochote kile kilichogusana nayo, na hivyo huu ni uthibitisho kua hairuhusiki kutumia Vijiwe kwa ajili ya Istijaa, kama vile inavyokubalika kwa ajili ya Mkojo na Kinyesi, hii ni kwa sababu ya kua mbali ya kua Hadith zote, ni zenye kutofautiana imaneno na kisanad, lakini hakunailiyotaja Vijiwe kwa ajili ya Istinja '**

Na kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi kama utakua na Maji kidogo sana basi hua unaruhusika kwanza kujipangusa kwa Tissue au Vijiwe n.k na kisha kumalizia kwa Maji.

Lakini kama hua maji basi Na umetokwa na Madhii na ikawa hakuna Maji basi anaruhusika kujitoharisha kwa Kartasi au Tissue au Vijiwe n.k.

Ila sasa kartasi au tissue hizo zisiwe zile zenye Maji bali ziwe kavu kwani zenye Maji hua hazisafishi bali zinasambaza zaid Najis husika.Na hutakiwi kutumia Kitu ambacho kinaweza kuliwa.Na wala haitakiwi na ni haram kutumia sehemu ya kiungo cha mwili wa Mnyama ambae yuko hai, labda kama mkia wake n.k

Kwani anasema Imam Ibn Naqib Al Masri Al Shafii kua: '**Vijiwe hutosheleza Kujitoharisha ingawa hua ni bora kumalizia kukosha kwa maji, Na kitu chochote kinaweza kuchukua nafasi ya Kijiwe Ila kitu hicho kiwe ni Kigumu Yabisi, Kisafi na kinachoweza kuondoa Najis husika**. **Na kisiwe kitu ambacho kinastahiki kuheshimiwa, au chenye thamani au kinachoweza kulika'***(Umdat Saliq)*

Na inatakiwa Ujisafishe mara tatu kwa kutumia Tissue kavu tatu au mawe matatu tofauti, au sehemu tatu tofauti za Tissue au jiwe hata kama kwa mara moja tu Najis hio itaondoka. Kwani kuna hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا أَبُو نُعَيْمٍ، قَالَ حَدَّثَنَا زُهَيْرٌ، عَنْ أَبِي إِسْحَاقَ، قَالَ لَيْسَ أَبُو عُبَيْدَةَ ذَكَرَهُ وَلَكِنْ عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ الأَسْوَدِ عَنْ أَبِيهِ، أَنَّهُ سَمِعَ عَبْدَ اللَّهِ، يَقُولُ أَتَى النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم الْغَائِطَ، فَأَمَرَنِي أَنْ آتِيَهُ بِثَلاَثَةِ أَحْجَارٍ، فَوَجَدْتُ حَجَرَيْنِ، وَالْتَمَسْتُ الثَّالِثَ فَلَمْ أَجِدْهُ، فَأَخَذْتُ رَوْثَةً، فَأَتَيْتُهُ بِهَا، فَأَخَذَ الْحَجَرَيْنِ وَأَلْقَى الرَّوْثَةَ وَقَالَ " هَذَا رِكْسٌ ".

Amesema Abu Nuaym kua ameseam Zuhayr kua amesema Abi Is-haq kua amesema si Abu Ubaydat aliesema bali ni Abdu Rahman Ibn Al Aswad kua amesema Baba yake kua amesema Jabir Ibn Abd *Allah Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alienda kujisaidia na kisha akaniomba mimi nimpelekee vijiwe vitatu.

Nikatafuta Na kupata Vijiwe viwili nikatafuta cha tatu nikakosa hivyo nikachukua Kinyesi cha Mnyama Kilichokauka badala yake na kumpa. ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akachukua Vijiwe viwili na kisha akakirembea Kinyesi kikavu huku akisema: 'Hiki ni Kitu Kichafu.''***(Sahih Bukhari)*

Na amesema Imam Abu Bakr Ibn Abi Shaybah kua wamesema Abu Muawwiyah na Waki Ibn Jarah kua amesema Al Amash. Na Yahya Ibn Yahya amesema pia amesema Abu Muawwiyah kua amesema Abd Rahman Ibn Yazid kua aliambiwa Salma Al Farsi *Radhi Allahu Anhu na Mayahudi* kua:

قِيلَ له: قدْ عَلَّمَكُمْ نَبِيُّكُمْ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ كُلَّ شيءٍ حتَّى الخِرَاءَةَ قالَ: فقالَ: أجَلْ لقَدْ نَهانا أنْ نَسْتَقْبِلَ القِبْلَةَ لِغائِطٍ، أوْ بَوْلٍ، أوْ أنْ نَسْتَنْجِيَ باليَمِينِ، أوْ أنْ نَسْتَنْجِيَ بأقَلَّ مِن ثَلاثَةِ أحْجارٍ، أوْ أنْ نَسْتَنْجِيَ برَجِيعٍ، أوْ بعَظْمٍ.

'Mtume Wenu amekufundisheni kila kitu hadi namna ya kujisaidia Haja kubwa. Hivyo Nami nikasema: 'Naam ametukataza mambo kama kuelekea katika Upande wa Kibla katika wakati wa Kujisadia haja ndogo na kubwa, Au kutojisafisha kwa kutotumia mikono ya Kulia, na Kujitojarisha kwa Vijiwe visivyopungua vitatu, na kutoharisha kwa kutumia Kinyesi kikavu au Mifupa.''*(Sahih Muslim)*

Ambapo anasema wa Imam Ahmad Ibn Muhammad Al Qastallani Al Shafii kuhusiana na hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akingia Chooni, na kisha mimi na mfanyakazi tulikua tukimletea Maji, na alikua akijitoharisha**

kutokana nayo' kua Hadith hii inapingana na na wale wasiopenda kujitoharisha kwa kutumia Maji na pia wale wanaokataa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifanya hivyo kujitoharisha kwa kutumia Maji.

Wakishikamana na kile kilichonukuliwa na Imam Ibn Shaybah huku kikiwa na Sanah iliyokua Sahih kabisa kutokea kwa Hudhayfa Ibn Al Yaman *Radhi Allahu Anhu* alipoulizwa kuhusiana na kujitoharisha na Maji ambapo nae akasema: 'Mikono itabakia na Harufu ya Kinyesi baada yake.'

Na imenukuliwa kutoka kwa Nafii kutoka kwa Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua hakua ni mwenye kujitoharisha na Maji' na imenukuliwa kutoka kwa Imam Al Zuhri akisema: 'Hatukua tukifanya hivyo' na imenukuliwa kutoka kwa Sayyid Ibn Musayyib kua aliulizwa kuhusiana na Kujitoharisha kwa Maji ambapo nae akasema kua: 'Huko Ni kujitoharisha kwa Wanawake.'

Na Imam Ibn Al Tin aenukuu kutoka kwa Malik ambae amekanusha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alijitoharisha kwa Maji, na imenukuliwa kutoka kwa Ibn Habbib ambae ni mmoja kati ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik kua amekataza kujitoharisha kwa Maji kwa sababu hua yana uwezo wa kubeba Maradhi ya kuambukiza. Na baadhi yao wamesema kua: 'Haikubaliki kujitoharisha kwa Mawe wakati inapokua Maji yapo'

Hivyo Sunna imetoa maamuzi kwa ajili yao, kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitumia Vijiwe na Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* alikua pamoa nae na alimpelekea bilauri la Maji pia. Na wengi mingoni mwa Wanazuoni wa mwanzoni wa Uislam wamekubaliana kua Kujitoharisha kwa Maji na Vijiwe hu ani bora zaidi, yaani Vijiwe vitumike mwanzo kupunguza Uchafu wa Najis na ugumu wa kugusa Najis kwa Mikono, na kisha maji yatumike na hii ni kwa haja zote za Kinyesi na Mkojo.*(Irshad Sarii Ala Sharh Sahih Bukhari)*

Na amesema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua**: 'Mtu mwenye Tumbo Dogo au Kubwa hua natakiwa ajisafishe kwa Vijiwe au kitakachoweza kuchukua nafasi yake. Pale itakapokua uchafu hautoweza kutapakaa zaidi ya sehemu uliyotokea, na ni ilikua ni kawaida kuwepo kwa watu wenye Matumbo madogo na matumbo makubwa, ila nadhania kua kwa Muhajirrin wengi ilikua ni wenye Matumbo madogo, na hii ni kutokana n akua wao walikua wakila sana Tende, na walikua wakila kama chakula chao hasa na ndio *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliwashauri kujisafisha kwa Vijiwe**'.*(Al Umm)*

Na katika hadithi nyengine imesemwa kua

حدثنا عبد الله بن محمد النفيلي حدثنا ابن المبارك عن محمد بن عجلان، عن القعقاع بن حكيم عن أبي صالح عن أبي هريرة قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: (إنما أنا لكم بمنزلة الوالد أعلمكم، فإذا أتى أحدكم الغائط فلا يستقبل القبلة ولا يستدبرها ولا يستطب بيمينه، وكان يأمر بثلاثة أحجار، وينهى عن الروث والرمة).

'Amesema Abd Allah Ibn Nufayl kua amesema Abd Allah Ibn Mubarak kua amesema Muhammad Ibn Ajlan kua amesema Ad Daqa' Ibn Hakim kua amesema Abu Salih kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua : Mimi ni kama Baba yenu na ni Mwenye Ilm kubwa zaid miongoni mwenu. Hivyo Mkijisaidia Haja kubwa basi msielekee Kibla, na Wala Msikipe Mgongo Kibla, na wala msijisafishe kwa

mikono ya Kulia, Mkijisafisha kwa vijiwe tumieni vijiwe visivyopungua Vitatu na msitumie Kinyesi kikavu wala Mifupa.'*(Sunnan Abu Daud)*

Hizi ni hadith zinazozungumzia kuhusiana adabu za kujisaidia kua ni kufanya I*stinja'* baada ya kumaliza kwa kutumia maji au Vijiwe visivyopungua vitatu kwa ajili ya kujitoharisha, na pia kutoelekea Kibla katika wakati wa kujisaidia pale Mtu unapojikuta umeshikwa na haja halafu ikawa uko nje, kama Jangwani, Msituni, Baharini n.k kwa sababu hua hakuna kitu kinachoweza kukuwekea mpaka wa kukuhifadhi kutokana na upande wa Kibla.

Lakini kama ikiwa ni nyumbani kwako basi hua hamna tatizo kama ilivyosemwa katika hadith ya Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* iliyonukuliwa na Marwan Ibn Al Asfar kua:

«رأيتُ ابنَ عمرَ أناخَ راحِلتَه مُستقبِلَ القِبلةِ، ثُمَّ جَلَسَ يَبولُ إليها، فقلتُ: يا أبا عبدِ الرَّحمنِ، أليسَ قد نُهِيَ عن هذا؟ قالَ: بلى، إنَّما نُهِيَ عن ذلك في الفَضاءِ، فإذا كانَ بينَك وبين القِبلةِ شيءٌ يَستُرُك فلا بأسَ»

Nilimuona mimi Ibn Umar akiinamisha Kipando chake kuelekea Kibla na kisha akashuka chini na kuchutama na kujisaidia haja ndogo, hivyo nami nikasema: Ya Abu Abd Rahman, hivi Jee haijakatazwa kufanya hivyo?.

Ambapo nae akasema: 'Naam, imekatazwa pale inapokua uko katika sehemu iliyokua wazi, lakini kama ikiwa kuna kitu kitakachokuzinga baina yako na Kibla basi hua hamna tatizo.'

Na imekatazwa kutumia kinyesi kikavu cha Mnyama kwa sababu Kinyesi huya ni Najis, na imekatazwa kutumia Mifupa kwa sababu ya hadith ya Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*isemayo kua:

عن عامر، قال: سألتُ عَلْقَمةَ: هل كان ابنُ مسعود شَهِدَ مع رسول الله صلى الله عليه وسلم ليلةَ الجنِّ؟ قال: فقال عَلْقَمةُ، أنا سألتُ ابنَ مسعود فقلتُ: هل شَهِدَ أحدٌ منكم مع رسول الله صلى الله عليه وسلم ليلةَ الجنِّ؟ قال: لا، ولكنَّا كنَّا مع رسول الله ذاتَ ليلة ففَقَدْناه فالتمسناه في الأودية والشِّعاب. فقلنا: استُطِير أو اغْتِيل. قال: فبِتْنَا بِشَرِّ ليلة بات بها قومٌ، فلما أصبحْنا إذا هو جاء من قِبَل حِرَاء. قال: فقلنا يا رسول الله فقدْناك فطلبْناك فلم نجدْك، فبِتْنَا بِشَرِّ ليلة بات بها قوم. فقال: «أتاني داعي الجنِّ فذهبتُ معه فقرأتُ عليهم القرآنَ» قال: فانطلقَ بنا فأرانا آثارَهم وآثارَ نِيرانِهم وسألوه الزاد فقال: «لكم كلُّ عظم ذُكر اسمُ الله عليه يقع في أيديكم أوفر ما يكون لحمًا، وكلُّ بَعْرة عَلَفٌ لدوابِّكم» . فقال رسول الله صلى الله عليه وسلم : «فلا تسْتَنْجُوا بهما فإنَّهما طعامُ إخوانِكم.

Kutoka kwa Amar amesema kua: Nilimuuliza Alqamah: 'Je, Ibn Masoud alikuwepo pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*katika usiku wa majini?

Alqamah amesema, nilimuuliza Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu*na kusema: Je, kuna yeyote kati yenu aliyeshuhudia Usiku wa Majini pamoja na*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. '

Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* Akasema: 'Hapana, lakini tulikuwa pamoja na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Usiku mmoja tukampoteza, na tukamtafuta mabondeni na mabondeni. Tukasema: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* itakua amepeperushwa au ameuawa.

Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akasema: Basi tukakaa usiku ambao ulikua ni Usiku mbaya kabisa kuwahi kupitiwa na watu, na tulipoamka asubuhi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*akaja kutoka upande wa Hira. nasi tukasema, Ya Rasul Allah?, tumekukosa na tukakutafuta lakini hatukukupata, basi tukakaa usiku mbaya kabisa ambao watu wowote wamewahi kuutumia.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Alinijia mwitaji wa majini, na nikaenda nae na nikawasomea Qur'ani.'**

Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* akasema: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaondoka pamoja nasi na akatuonyesha athari zao na athari za moto wao, Na wakamuomba riziki, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*a akawaambia Majini hao kua : 'Kila mfupa ambao umetajwa jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* ukianguka mikononi mwenu utakuwa na nyama nyingi zaidi, na kila kipande cha Kinyesi kitakuwa chakula kwa ajili ya wanyama wenu.'' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. akasema: 'Hivyo msivitumie kwa ajili ya kujitoharishia kwanini chakula chao, kwani ni ndugu zenu''.

Ambapo kwa upande mwengine basi Imam Ibn Al Qayyim amemnukuu Imam Abu Hafs Al Barmaki Al Hanbali katika *Badai Al Fawaid* kwa kusemakua: **'Inatosheleza kujimwagia Maji kutokana na Madhii, kwa sababu Madhii si Najis na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: Haya ni Manii ya Farasi Dume na kila Farasi Dume hua ana Manii yake' hivyo kutokana na kua Manii ya Farasi Dume hua ni Tohara basi hua na Madhii pia kwa sababu yote hua yanatokana na Matamanio.'**

Na tunapoangalia kitabu cha Muwwata cha Imam Malik basi tunaona kuna mlango wa *Kuruhusika Kutotia Udhuu Baada ya Kutokwa na Madhii* ambamo ndani yake Mna hadith isemayo kua;

'Amesema Yahya Ibn Said kua amemsikia Said Ibn Al Musayyib akiulizwa suali na Mtu kwa kusema kua: 'Nnahisi umaji maji wakati nikiwa nnasali, hivyo jee nisisali?' Said Ibn Musayyib akasema: Hata kama yakitiririka kwenye Mapaja yangu basi mimi sitokatisha Sala hadi nitakapoimaliza' *'(Muwwata Imam Malik)*

Na Imam Ibn Abi Shaybah amesema kua: '**Amesema Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Yahya Ibn Said kua amesema Said Ibn Musayyib kua: 'Mimi nnahisi kua Madhii yanatiririka kwenye Mapaja yangu, wakati nikiwa nnasali lakini sijali juu yake.'**

Na amesema Said Ibn Musayyib kua alisema Umar Ibn Al Khattab kua: 'Mimi nilihisi Madhii yananitiririka kwenye Mapaja yangu wakati nilipokua kwenye Minbari lakini sikujali'

Na amesema Imam Sufyan Ath Thawry kua: 'Amesema Yahya Ibn Said kua amesema Said Ibn Musayyib kua: 'Hata kama Madhii yakinitiririka kwenye Mapaja yangu, basi sitokatisha Sala''

Na amesema Imam Ibn Uyaynah kua amesema Ibn Ajlan kua: 'Nimemsikia mimi Abd Rahman Al Araj akisema kua: 'Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* alisema wakati akiwa kwenye Miinbar kua: Kuna kitu kama Lulu au Shanga kinatiririka kwenye Mapaja yangu, na sijali kuhusiana nayo''*(Musannaf Ibn Abi Shaybah)***

Na amesema Imam Al Rafii Al Shafii kua: **'Mtizamo uliokua sahih kabisa ni kua Mtu hua anaweza kuchagua baina ya kukoga Janaba na kuchukulia kua ni Manii au kutia Udhu' na kuchukulia kua ni Madhii na hii ni kwa sababu inawezekana ikawa ni kioja kati ya vitu viwili hivyo, hivyo kama akijitoharisha kwa njia moja wapo, basi Sala yake itakua sahih kwa sababu umuhimu wake umetokana na kua na shaka ambapo asili yake ni kutokwepo kwake.'***(Fat-h Al Aziz)*

Na kwa upande wa Al Muhaqqiq Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Kama ikiwa Mtu ana shaka kuhusiana na kitu Fulani, kua labda kitu hicho ni Madhii au ni Manii, basi hu ana hiari hata kama ikiwa ni kutokana na matamanio, hivyo akitaka anaweza kuchukulia kua ni Manii na kisha akakoga Janaba au akachkulia kua ni Madhii na akayakosha kwa maji tu, Na kisha akatia Udhu.'**

'Na hii ni kwa sababu kama akifanya moja kati ya mambo mawili hayo, hua in mwenye kua na shaka kutokana na lile ambao hakulifanya, na kilichokua na shaka hua hakina wajibu juu yake. Kwani hata Mtu aliesahau moja kati ya Sala mbili basi hu ana Wajibu wa kuzisali zote katika wakati wa kipidi cha Sala moja, kwa sababu ya kua na uhakika ni Sala za Fardh juu yake, hivyo hatakiwi kuachana nazo isipokua kutokana na kua na uhakika kua amezisali'*(Tuhfah Al Muhtaj)*

Na Anasema Imam Al Shirbini Al Shafii kua: '**Kama ikiwa Mtu atafanya kile kinachotakiwa kati ya kimoja miongoni mwa hivyo, basi Shaka yake itakua imeondoka, na kanuni ya msingi hu ani kua Udhuu wake utakuwepo kutokana na kutekelezea kimoja miongoni mwao na hivyo hakuna kitakachopingana na tohara yake hio, hii hu an tofauti na mtu ambae amesahau moja katia ya Sala mbili ambapo hu aanatakiwa kuzisali zote Mbili kwa sababu ufahamu wake umechukuliwa na Sala zote mbili na hivyo Sala zote mbili hua zipo, hivyo kama akiisali moja wapo basi Sala hio hua inahesabiwa, lakini kama hakuisali basi hua anatakiwa kuisali Sala hio na inayofuatia'(***Al Iqna)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA UDHU- MADHII YA MWANAMKE

❖❖❖❖

Kama tunavyoona katika Hadith mbali mbali kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivyokua akijitahid kuufundisha Ummah wake kuhusiana na kila kitu kinachohusiana na Mfumo wa Maisha aliyoupanga Muumba ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa kutuwekea Njia ya Dini ya Kiislam.

Ambapo ndani yake mna Adabu za juu ya kila kitu katika Maisha hadi namna ya Kujisaidia, Kula, Kuingiliana na Wenza wetu, Kujitoharisha, Kuvaa, n.k. Kiasi ya kua Makafiri wakawa wanawadhihaki Masahaba *Radhi Allahu Anhum* kuhusiana na mafundisho hayo kua Watu wamekua Wajinga hawajui kitu na hivyo Wanafundiwa hadi namna ya Kujisaidia.Lakini kutokana na Hikma na Ufaham waliokua nao Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na Mahaba kwa Nabii Muhammad S*alallahu Alayhi wa Salam* na Imani Thabit ya Dini ya Kiislam.

Basi Masahaba hawakukasirika walipokua wakidhihakiwa juu ya Dini hao bali waliona Ufahari, na hivyo kuzidi kufafanua kuhusiana na Uzuri wa Mfumo wa Maisha wa Dini ya Kiislam. Hivyo nasi tuko

katika kukumbushana kuhusiana na Adabu za Tohara za Kiislam kuhusiana na yale yanayobatilisha Udhu na Sala.

Kama vile walivyokua wakikumbushana waliotangulia kabla yetu kuhusiana nayo, na ingawa ndani yake mna mambo ambayo kwa baadhi wanaweza kuona kua hayafai kuyazungumzia kwa kina kama kuhusiana na Manii, Madhii ya Wanawake na Unyevunyevu wa Kimaumbile wa Uke.

Lakini hata hivyo Haya ni miongoni mwa mambo ambayo ndio chanzo cha Asili ya Maisha ya Kila Ibn Adam na hivyo yanatakikana kujulikana na kuzungumziwa na kukumbushana juu yake. Kwani hata Qur'an na Hadith zimeyazunguzia juu yake.

Na Maimamu kama kina Hujjat ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali Al Shafii ameyazungumzia katika Ihya Ulum Ad Din, Imam Ibn Al Jawzi katika Sauf Al Khatir, Imam Ibn Al Qayyim ameyazungumzia kwenye Tibb An Nabawi,Imam An Nawawi katika Al Majmuu, Imam An Nasai katika Ishrat Al Nisai,Imam Ibn Qudamah katika Al Mughni, Imam Ibn Abidin,n.k.

Hivyo haya si mambo ya kuficha na kuoneana haya kuyazungumzia bali ni ya kuyaweka wazi na inabidi tukumbushane kwani amesema Imam Mujahid kua: **'Ilm yenye Manufaa haiwezi kupatikana kwa Mtu mwenye Kuona Haya au mwenye Kibri.'***(Sahih Bukhari)*

NaImam Muslim amesema kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ الْمُثَنَّى، وَابْنُ، بَشَّارٍ قَالَ ابْنُ الْمُثَنَّى حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ جَعْفَرٍ، حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، عَنْ إِبْرَاهِيمَ بْنِ الْمُهَاجِرِ، قَالَ سَمِعْتُ صَفِيَّةَ، تُحَدِّثُ عَنْ عَائِشَةَ، أَنَّ أَسْمَاءَ، سَأَلَتِ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم عَنْ غُسْلِ الْمَحِيضِ فَقَالَ " تَأْخُذُ إِحْدَاكُنَّ مَاءَهَا وَسِدْرَتَهَا فَتَطَهَّرُ فَتُحْسِنُ الطُّهُورَ ثُمَّ تَصُبُّ عَلَى رَأْسِهَا فَتَدْلُكُهُ دَلْكًا شَدِيدًا حَتَّى تَبْلُغَ شُئُونَ رَأْسِهَا ثُمَّ تَصُبُّ عَلَيْهَا الْمَاءَ . ثُمَّ تَأْخُذُ فِرْصَةً مُمَسَّكَةً فَتَطَهَّرُ بِهَا " . فَقَالَتْ أَسْمَاءُ وَكَيْفَ تَطَهَّرُ بِهَا فَقَالَ " سُبْحَانَ اللَّهِ تَطَهَّرِينَ بِهَا " . فَقَالَتْ عَائِشَةُ كَأَنَّهَا تُخْفِي ذَلِكَ تَتَبَّعِينَ أَثَرَ الدَّمِ . وَسَأَلَتْهُ عَنْ غُسْلِ الْجَنَابَةِ فَقَالَ " تَأْخُذُ مَاءً فَتَطَهَّرُ فَتُحْسِنُ الطُّهُورَ – أَوْ تُبْلِغُ الطُّهُورَ – ثُمَّ تَصُبُّ عَلَى رَأْسِهَا فَتَدْلُكُهُ حَتَّى تَبْلُغَ شُئُونَ رَأْسِهَا ثُمَّ تُفِيضُ عَلَيْهَا الْمَاءَ " . فَقَالَتْ عَائِشَةُ نِعْمَ النِّسَاءُ نِسَاءُ الأَنْصَارِ لَمْ يَكُنْ يَمْنَعُهُنَّ الْحَيَاءُ أَنْ يَتَفَقَّهْنَ فِي الدِّينِ .

Asma Bint Shakal alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Tohara ya baada ya kumaliza siku zake za Hedhi. Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia kua: 'Kila mmoja miongoni mwenu anatakiwa atumie maji yaliyochanganywa na Majani ya Mkunazi na kisha ajimwagie kichwani na kujisugua hadi ahakikishe kua mizizi yote ya nywele zake imeguswa na maji, na kisha ajimwagie Maji mwili mzima'

'Na kisha achukue kipande cha pamba chenye Miski na Kisha AJitoharishe kutokananacho' Asma akauliza: 'Sasa Mtu atajitoharisha vipi kutokana nacho?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akamwambia: 'Subhanah Allah, atajitoharisha kutokana nacho.'**

Aisha *Radhi Allahu Anha*akasema kwa sauti ya chini kua akichukue kisha ajipake kufuatisha sehemu zilizoathirika kwa Damu.'

Kisha Asma akamuuliza*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*kuhusiana na kujitoharisha kutokana na Janaba. *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia : 'Chukua maji yako, kisha jitoharishe nayo vizuri sana kwa kadiri utakavyoweza. Kisha jimwagie kichwani na ujisugue hadi uhakikishe kua kila mzizi wa nywele zako kua umeroa. Kisha jimwagie Maji mwili mzima.'

Hivyo Aisha *Radhi Allahu Anha*akasema kua: '**Wanastahiki Pongezi Wanawake wa Kiansari kwa sababu Hisia za Haya hazikuwazuia wao kuuliza masuali kwa kina katika kutaka kuifahamu Dini ya Kiislam.'***(Sahih Muslim)*

Naam...kama tulivyoona hapo kabla katika Kua amesema Mujtahid Imam Al Madhhab Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: **'Kila Kitakachotoka kwenye Sehemu za Siri za Mwanamme iwe Mkojo,Madhii, Madii au kitu chochote kile kisichojulikana hua ni Najis. Isipokua Manii.'***(Al Umm)*

Hivyo ingawa hukmu hii inazungumzia kuhusiana na kitakachotoka kwenye Sehemu za Siri za Kiume kua ni Najis lakini hapo hapo kulingana na Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi Hukmu hii hua inawahusu na Wanawake pia, isipokua kwa upande wa Wanawake basi inabidi kuna Ufafanuzi wa zaidi kutokana na Utofauti wa Kimaumbile baina ya Wanawake na Wanaume, kama ilivyosema Hadith tuliyoiangalia hapo kabla ya Aisha R*adhi Allahu Anha*isemayo kua:

سُئلَ رسولُ اللَّهِ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ عنِ الرَّجلِ يجدُ البللَ ولا يذكرُ احتلامًا ؟ قالَ : يغتسِلُ وعنِ الرَّجلِ يرَى أنَّهُ قد احتلمَ ولم يجِدْ بللًا قالَ لا غُسلَ عليهِ قالت أمُّ سلمةَ يا رسولَ اللَّهِ هل علَى المرأةِ ترَى ذلِكَ غُسلٌ قالَ نعَم إنَّ النِّساءَ شقائقُ الرِّجالِ.

'***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **aliulizwa kuhusiana na Mtu aliona unyevunyevu kwenye Mwili wake na Nguo zake, lakini hakua ni mwenye kukumbuka Kuota kuhusiana na Kuingiliana kimwili.**

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Inambidi Mtu huyo Kukoga.'

Na akaulizwa tena kuhusiana na Mtu ambae anakumbuka kua aliota Ndoto ya kuingiliana ndani yake lakini Hakujikuta kua ameroa.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema kua: 'Haimlazimu Mtu huyo Kukoga.'**

Na kisha Ummu Salamah akauliza: 'Je na Mwanamke akiona hivyo hua ni Wajibu kukoga pia?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: 'Naam, Wanawake ni wenza wa Wanaume.'***(Sunnan Abu Daud)*

Ambapo kuhusiana na Manii ya Wanawake basi hua ni kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Manii ya Wanawake basi hua na Unjano njano na wepesi, na pia huweza kua na weupe ambapo hii hua ni kulingana na uwezo wa Kinguvu wa Mwanammke husika.**

Na amesema Imam Al Haramayn na Imam Abu Hamid Al Ghazali kua Sifa kuu ya Manii ya Mwanamke hua ni Kuhisi hisia za Raha na Mmaliziko wa Hamu ya Mwanamke, baada ya kutoka Manii hayo, na hua hayajulikani isipokua kwa Dalili hizo.

Na akasema Imam Al Ruywani Al Shafii kua Manii ya Mwanamke pia hua na Harufu kama Manii ya Mwanamme.

Hivyo kutokana na vithibitisho hivi basi tunaona kua Manii ya Mwanamke yana sifa mbili na yanajulikana kwa moja kati ya mbili hizo.' (*Al Majmuu)*

Ambapo kuhusiana na Madhii ya Mwanamke ambaya kwa baadhihua wanayaita kua ni Qadhi kama ilivyosemwa kwenye Al Lisan kua: **'Kila Mwanamme hua anatokwa na Madhii nakila Mwanamke hua anatokwa na Qadhi'**

Nakama alivyosema Imam An Nawawi katika Al Majmuu kua: '**Ama kuhusiana na Madhii basi hua ni Majimaji mepesi meupe yenye utelezi ambayo humtoka anapokua na hamu, lakini hua bila ya hisia wala nguvu katika kutoka kwake na hayamsababishii uchovu wa mwili baada ya kutoka kwake Na hivyo kama ilivyo kwa Mwanamme basi na kwa Mwanamke hivyo hivyo hua hahisi utokwaji wa Madhii.**

Na Imam Al Haramayn amesema kua: Wakati Mwanamke anapokua na hamu ya Matamanio basi hutokwa na Madhii na kwa Wanawake hua ni mara kwa mara zaidi kuliko kwa Wanaume.'*(Al Majmuu)*

Ama kuhusiana na Madii basi Wanazuoni wanakubaliana kua ni Majimaji mazito kidogo yanayofuatia baada ya Kujisaidia Haja ndogo kwa upande wa Wanaume na Wanawake pia.Na kama tulivyoona kua Manii ya Mwanamme na Mwanamke hua ni Tohara kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal, ila huweza kua Najis kama yatakua yamechanganyika na Najis.Na ingawa Manii si Najis na hayabatilishi Udhu lakini Manii humuwajibisha yule yaliemtoka kua na Wajibu wa Kukoga Janaba.

Na kuhusiana na Madhii na Wadii ya Wanaume na Wanawake basi hua ni Najis na hivyo Hubatilisha Udhu na hivyo kumpelekea yule yaliemtoka Kujisafisha tu sehemu husika iliyoingia Madhii au Madii na Kutakiwa kutia Udhu kabla ya Kufanya Ibada ya Sala na Nyenginezo. Na bila ya shaka Madhii na Madii hua hayamuwajibishi kukoga yule yaliemtoka.

Wanazuoni wamehitilafiana kuhusu Madhii yanapokuwa nguoni, baadhi yao wanasema: Haifai nguo hiyo isipokuwa kwa kukoshwa, ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Al Shafii na Imam Is-haq Ibn Rahawayh kama alivyosema Imam An Nawawi katika *Sharh Al Muhadhdhab* kua:

'Kuna Makubaliano ya Wanazuoni kuhusiana na Madhii kua ni Najis, ambapo ni Najis ambayo mtu unaweza kujitoharisha nayo, na katika Skuli ya Madhhab yetu basi hua ni Wajibu kujitoharisha kwa kwa Kujikosha, au kukosha kitu husika kilichoingia Madhii, hivyo kumwagia mwagia maji tu hua haitoshelezi, nasi tunasimamia kwenye msingi wa Hadith ambayo imesema

kua *Yaghsilu Dhakarahu wa Yatawaddhau* yaani Akoshe Uume wake na Atawadhe'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na wengine wanasema kua Inatosha kunyunyizia maji ambao ni mtizamo wa Imam Ahmad Ibn Hanbal ambao nikua Kumwagia Maji tu sehemu iliyoingia Madhii hua inatosheleza kama ilivyosema hadith Sahl Ibn Hunayf kua:

كنتُ ألقَى مِنَ المذْيِ شدةً وعناءً ، فكنتُ أُكْثِرُ منه الغسلَ . فذكرْتُ ذلِكَ لِرَسولِ اللهِ صلَّى اللهُ - عليْهِ وسلَّمَ وسألْتُهُ عنْهُ ؟ فقال : إِنَّما يجزِئُكَ منْ ذلِكَ الوضوءُ فقلتُ يا رسولَ اللهِ ، كيْفَ بما يُصِيبُ ثوبِي منْهُ ؟ قال : يكفيكَ أنْ تأخُذَ كفًّا مِنْ ماءٍ فتنضَحَ بِهِ ثوبَكَ حيثُ ترَى أنَّهُ أصابَ مِنْهُ

Mimi nilikua ni Mtu ambae nna matatizo ya Kutokwa na Madhii sana, na hivyo ilikua kila wakati nnakoga Janaba.Hivyo nikamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana nayo ambapo nae akaniambia kua Udhu tu hua unatosheleza kwa Madhii. Hivyo nami nikamuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: Jee vipo kuhusiana na yataingia kwenye Nguo zangu?

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Itakutosheleza kama utachukua gao la Maji na kumwagia kwenye sehemu ya nguo yako ambayo unadhania kua imeingia Madhii.'(Sunnan Abu Daud, Sunan At Tirmidhii, Sunnah Ibn Majah, Sunan Ad Darimi Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo hadithi hii imetumia neno *Nadha* ambalo kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal ni lenye kumaanisha Kuwagia Maji, ambapo hata hivyo kwa upande wa Imam Muhammad Idris Al Shafii basi ni lenye kumaanisha aidha Kumwagia Maji Kitu au Kukikosha Kitu na hadiithi nyengineyo imeamrisha kukosha, hivyo maana ya neno hili katika hadith hii linamaanisha kukosha, kama alivyosema Imam An Nawawi kua:

فَإِنَّ النَّضْحَ يَكُونُ غَسْلًا وَيَكُونُ رَشًّا

Hakika ya *Nadhiha* hua ni aidha Kukikosha kwa Maji Kitu au Kukirashia Maji Kitu.*(Al Minhaj Sharh Sahih Muslim Bin Al-Hajjaj)*

Na imesema katika Nail Al Awtar kua: **'Kama Madhii yakimtoka Mtu na wakati wa Sala umeshawadia basi Mtu huyo hua anatakiwa akoshe sehemu yaliyoingia na pia atie Udhu.'**

Na kutokana na kua Madhiini Najis basi kama Madhii yataingia kwenye Nguo basi Nguo hio hua haifai Kusalia, kasema Imam Ibn Naqib Al Masri kua: **'Kama ikiwa Mtu ana uhakika juu ya kitu kilichoingia kwenye nguo yake ni Madhii, basi hua haruhusiki kusalia nguo hio iliyoingia Madhii hadi itoharishwe kwa sababu ya kua Madhii ni Najis'***(Umadat Al Salik)*

Na Imam Muhammad Ibn Abidin Al Shami anasema kwenye *Manhal Al Waridayn* kua: **'Kama ikiwa Mwanamke atakua na shaka kuhusiana na Madhii kutoka nje ya Labia kubwa basi hii itamaanisha kua hakutokwa nakitu, na hivyo ha haina haja kwake kuurudia Udhu, na haina haja ya kujichunguza zaidi.'***(Manhal Al Waridayn)*

Imam Ibn Abidin amezungumzia kuhusiana Labia kubwa kwa sababu kimaumbile Uke hua na Mashavu ya aina mbili ambayo ni Labia Ndogo na Mashavu ya Nje hua yaaitwa Labia Kubwa, Hivyo kama Madhii yatakua yanaonekana nje ya Labia kubwa basi Udhu hua unavunjika,

Na kwa upande wa Wanawake mbali ya kua wanatokwa na Manii, Madhii na Madii kama ilivyo lakini pia hua na Rutubat Al Faraj au Unyevunyevu wa Kimaumbile wa Uke.

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- RUTUBAT AL FARJ

❖❖❖❖

Kwa kimaumbile Wanawake hua wanatokwa na aina sita tofauti za Maji Maji kwenye uke ambazo hua ni tofauti kanisa na Manii na Madhii na huweza kutofautishwa kutokana na asili ya Rangi zake ambazo ni:

1-Maji maji Meupe yana uzito uzito kidogo ambayo hua ni Dalili ya Afya ya Kimaumbile ya Uke ingawa baadhi Ya Wakati Hua yanaashiria pia kuna tatizo la Uchachu wa Uke (Yeast Infection) pale yanapokua na muasho.

2-Majimaji ya Rangi ya Manjano ambayo husababiswa na Maradhi ya Maambukizi ya Uasharati kama yatakua yana harufu na kama hayana harufu basi hua hakuna tatizo.

3-Maji Maji Mekundu ambayo hua ni Damu ya Hedhi, Au Istihadhah, au Tatizo la Kizazi kama Saratani n.k.

4-Maji Maji ya rangi ya Pink ambayo husababishwa na Jeraha la Mfuko wa Uzazi au Uke.

5-Maji Maji rangi ya Kijivujivu ambalo humaanisha Tatizo la Bakteria.

6-Maji Maji yasiyokua na Rangi kabisa ambayo yana Utelezi fulani hivi ambayo Husababishwa na Afya ya Uke Kimaumbile katika wakati wa Kati kati wa Mzunguko wa Mwezi katika Kipindi cha Kuzalishwa kwa Yai la Uzazi, au kutokana na Kua na Ujauzito, au kutokana na mparaganyiko wa Uzalishwaji wa Kemikali za Mwili.

Ambapo rangi na hali ya Majimaji haya hua yanaweza kubadilika kutokana na athari ya Matumizi ya Dawa fulani kulingana na maumbile ya Mwanamke husika.

Na kutokana na kua Kimaumbile Majimaji haya hua ni moja kati ya sehemu ufanyajikazi kamilifu wa Mwili wa Ibn Adam Mwanamke, kama mmoja kati ya mfumo wa Usafishaji na Uboreshaji wa Uke Kiafya kwa ajili ya Uzazi basi hua ni yenye kuzalishwa kila wakati ndani ya Uke.

Kwani hua ni yenye kuzipa Ulinzi sehemu za Siri za Uke kwa Kuzipa unyevunyevu ambao huzuia sehemu za ndani za Uke kutochunika kwa kuzilainisha.Na kwa kua Hifadhi na Ulinzi wa Sehemu za Siri za Uke na Kizazi ndio kazi yake basi mabadiliko ya Muonekano wake pia hua ni wenye kuashiria juu ya athari za tatizo katika sehemu hizo ambako nako kutampelekea Mwanamke husika kuchukua hatua stahiki ili kutibu tatizo husika ndani ya mwili wake.

Na bila ya shaka kwa Upande wa Mitizamo ya Madhhab ya Fiqh basi Majimaji haya yote hua yanajulikana kama *Rutubat Al Farj* yaani Majimaji au Unyevunyevu wa Uke.

Ambapo anasema Imam Abd Rahman Ibn Muhammad Ibn Husayn Ba Alawi kua: **Rutbah Al Farj hua ni Maji Maji meupe ambayo yana muonekano wa kati na kati baina ya Madhii na Jasho, na**

Wanawake hua nayo kutokana na sababu za Kimaumbile na pia bila sababu yeyote Hivyo Hukmu yake kuhusiana nayo hua ni kama ifuatavyo:

1-Kama maji maji haya yatakua yanatoka nje ya Uke, basi Maji hayo yatakua Tohara na hayabatilishi Udhu.

2-Kama yatakua yanayoka Ndani ya Uke basi yatakua Tohara lakini yanabatilisha Udhu, hivyo Mwanamke atatakiwa atie udhu kila yatakapomtoka, lakini hatokua na haja ya kukosha Nguo yake ya ndani isipokua pale atakapokua na uhakika kua Maji hayo yametoka ndani kwenye Mfuko wa Uzazi, kama vile maji ya Uzazi ambapo yatakua si tohara na hivyo itambidi akoshe nguo yake.

3-Na kama Mwanamke hana uhakika kua kama Maji hayo yametoka nje ya Uke ama ndani basi itambidi ahesabu kua ni Tohara,na Udhu wake haujakatika kwa sababu shaka haiibatilishi Hakika.

Na inabidi tujue kua tunapozungumzia kuhusiana na sehemu ya Nje ya Uke basi hua tunazungumzia sehemu ambayo hua inaonekana pale Mwanamke anapochutama kujisaidia, na sehemu ya ndani hua ni sehemu iliyo ndani yake na isiyoonekana. Hivyo ndivyo walivyokubaliana Wanazuoni wetu.'*(Bughyat Al Mustarshidin)*

Kwani anasema Imam Al Muhaqqiqin Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: '***Rutbat Al Farj* hua ni Majimaji meupe yaliyokua katika hali ya baina ya Madhii na Jasho ambayo hutoka Ndani ya Sehemu isyokosheka ya Uke Na hivyo hua ni Tofauti Majimaji yanayokuwepo kwenye sehemu inayokosheka ya Uke, ambayo hua ni Tohara.'***(Tuhfah Al Muhtaj)*

Naam..hii ni moja kati ya Fatwa kuhusiana na *Rutbat Al Farj* kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kama tulivyoona katika Hukumu ya Asili ya Imam Muhammad Idris Al Shafii iliyosema kua: **'Kila kitokacho katika Uchi hua ni Najis isipokua Manii.'**

Na Imam Sulayman Al Bujaraimi Al Shafii ameifafanua Fatwa hii ya ImamIbn Hajar Al Haytami kwa kusema kua: '**Tunatakiwa Tufahamu kua Majimaji yanayotoka katika Uke hua yamegawika katika Makundi Matatu ambayo ni:**

1-Majimaji yaliyokua Tohara bila ya kua na shaka yeyote hua ni yale Majimaji au Unyevunyevu yanayotoka katika sehemu ambazo hua zinaonekana pale Mwanamke anapochutama

2-Maji Maji ambayo kwa ujumla ni Tohara ambayo ni yale yanayofikia katika Mlango wa kuingilia Ndani ya UkeYaani katika sehemu ambayo tendo la Kuingiliana hua linatokea

3-Majimaji au Unyevunyevu ambao Bila ya shaka hua si Tohara ambayo hua ni yale yanayoanzia Ndani zaidi ya Mlango wa Uke.'*(Hashiyah Al Bujaraimi)*

Kwa Maana hio basi kama ikiwa Mwanamke atakua hajui Unyevunyevu huo umetokea wapi basi hua anatakiwa ahesabie kua ni wa Nje nje na hivyo Utohara wake wa kua na Udhu haujatenguka, ila kama ikiwa ana uhakika ni wa kutokea ndani basi Udhu utabatilika

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi basi yeye anasema kua:

Rutubat Al Farj **-Unyevunyevu wa Uke hua ni Majimaji meupe na bila ya shaka hua na hali ya baina ya Madhii au Jasho.**

Hivyo Wanazuoni wametufautiana Kimtizamo kuhusiana nayo na Hukmu zake. Hivyo (Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii) Muandishi wa Kitabu hiki cha Al Muhadhdhab na ndie pia Muandishi wa kitabu cha Al Tanbih amefikiri kua Rutubat Al Farj sio Tohara,ambapo Mtizamo huo pia umechaguliwa na Imam Al Bandaniji Al Shafii.

Lakini Mtizamo wa Imam Al Baghawi (Al Shafii) na Imam Al Rafii (Al Shafii) ambao ndio Sahih kabisa ni ule usemao kua Rutubat Al Farj ni Tohara.

Na mwandishi wa Al Hawi (Imam Al Mawardi Al Shafii) amesema hivyo (Rutubat Al Farj Ni Tohara) katika Mlango wa Yale yanayowajibisha Kukoga Janaba juu yake Na Imam Al Shafii ametilia Mkazo juu ya Utohara wa Rutubat Al Farj katika Vitabu vyake.'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na tunaporudi kwa Muandishi wa Kitahu cha Al Hawi Al Kabir alienukuliwa na Imam An Nawawi katika Fatwa yake ambae ni Al Qadhi Al Faqih Al Allamah Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii basi yeye amesema kua: '**Ama kuhusiana na na *Rutubat Al Farj* basi kuna Mitizamo Miwili juu yake ambapo mmoja miongoni mwao ambao ndio Mtizamo Sahih kabisa wa Skuli ya Madhhab yetu ya Imam Al Shafii basi ni Kua *Rutubat Al Farj* ni Tohara**.'(*Al Hawi Al Kabir)*

Na akasema tena Imam Sulayman Al Bujaraimi kua: '***Rutubat Al Farj*** **au Unyevunyevu wa Uke ambyo hua ni Majimaji yanatoka kwenye Uchi wa mbele wa Mwanamke hua ni Tohara na Haubatilishi Udhu.**

Kwani Unyevunyevu huu hua unasababishwa na Jasho litokalo katika sehemu ya Nje ya Uke ambayo hukutana na Uume katika wakati wa Mwanamke kuingiliana na Mwanamme, na Mtizamo sahih zaidi ni kua *Rutubat Al Farj* ni Tohara.'*(Hashiyah Al Bujaraimi)*

Na kwa upande wa Imam Sulayman Ibn Umar Al Jamal Al Shafii basi amesema pia kua: '***Rutubat Al Farj*** **hua ni Unyevunyevu unaotoka kwenye eneo la Uke ambalo hua ni Wajibu kulikosha, hivyo sehemu hio hua haiuchafui Uume kwa sababu sehemu hio hua ni Safi.'***(Hashiya Al Jamal)*

Na amesema Imam Abd Al Hamid Al Sharwani Al Shafii katika Kufafanua Fatwa ya Imam Ibn Hajar Al Haytami kua:

Wanazuoni Wanakubaliana kuhusiana na aina Tatu za Rutubat Al Farj ambazo ni:

1-Farj Al Kharij -Maji Maji ya sehemu ya Nje ya Uke, ambayo ni Tohara na Haibatilishi Udhu.

2-Farj Al Dakhil Maji yanayozalishwa Kuanzia kwenye Mlango wa Uke kuingia ndani.

Ambayo kulingana na Mtizamo unaokubaliza zaidi ni kua nayo pia ni Tohara na Hayabatilishi Udhu.

3-Maji yanayozalishwa Ndani zaidi ya Farj Al Dakhil ambayo hua Si Tohara na hivyo Yanabatilisha Udhu.'*(Tuhfah Al Muhtaj Fi Sharh Al Minhaj wa Hawashi Al Sharwani wa Al Abadi)*

Al-Allamah Al Imam Al-Kurdi Al Shafii anasema kua: **‘Kama nilivyoelezea katika ufafanuzi wangu ndani ya Al Irshad, na katika Al Abbab kua kilicho Najis katika Rutubat Al Farj ni kile kilichothibitishwa kua kimetoka ndani kabisa nyuma ya Uke.’**

Ambapo kwa Upande wa Al Muhaqqiq Imam Ibn Aabidin Al Shami Al Hanafi basi anasema kua: *‘***Ama kuhusiana na Farj Dakhila -Majimaji ya kuanzia Kwenye Mlango wa Uke kuingia Ndani basi hua ni Tohara na hayabatilishi kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Hanifa, lakini kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Yusuf na Imam Muhammad Ibn Al Hasan ambao ni Wanafunzi wake Imam Abu Hanifa basi wanasema kua Si Tohara na yanabatilisha Udhu** *(Darr Al Mukhtar)*

Kisha baada ya kuelezea hayo basi Imam Ibn Abidin anarudi kwenye Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na kufafanua Mtizamo wa Imam Al Muhaqqiqin Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii na kusema kua: *‘***Hivyo kuhusiana na Rutubat Al Farj Al Kharij basi ni Tohara na hii ni kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni na kuhusiana na Rutubat Al Farj Al Dakhila basi kuna kutofautiana juu yake.***(Darr Al Mukhtar)*

Na kwa upande wa Imam Mansur Al Buhuti Al Hanbal basi anasema kua**: ‘Rutubat Al Farj ni Tohara kama vile ilivyothibitishwa Utohara wa Manii kwa sababu, kama ingekua Manii ya Mwanamke si tohara basi na Maji Maji ya Uke pia yangekua si Tohara.’***(Kashf Al Qina an Al Iqna)*

Na akasema tena Imam Al Buhuti Al Hanbali kua: **‘Wanazuoni wanasema kua Rutubat Farj Dakhil katika sehemu ambayo Muingiliano wa Kimwili baina ya Mwanamme na Mwanamke unatokea ni Tohara**. **Kama vile yalivyo Mate, Majasho, Mafua au Madenda yamtokauo Mtu wakati akiwa amelala.’***(Rawdha Al Murbi Sharh Zad Al Mustaqani, Al Risalah)*

Hivyo ingawa hio ndio mtizamo ya wengi zaidi miongoni mwa Wanazuoni lakini kwa upande wa Imam Al Khalil Ibn Is-haq Al Maliki Al Masri basi yeye amesema kua:**‘Rutubat Al Farj si Tohara kwa sababu ya kuchanganyika kwake na Mkojo na Najis nyenginezo.’***(Al Tawdhij Fii Mukhtasaf Ibn Hajib)*

Ambapo hata hivyo Mtizamo huu Umepingwa kwa sababu ya kuwepo kwa Utofauti wa Mlango wa Mkojo na wa Uke.

Hivyo basi kutokana na Mitizamo hii kabla ya kufafanua Vithibitisho vyao basi tunahitimisha kwa kukumbushana kua. Kama ikiwa Mwanamke atakua na Uhakika kua Maji Maji aliyoyaona kua ni yenye Kutoka Juu Kwenye Mlango wa Uke, au kwa ndani Kidogo ya Uke basi Maji Maji hayo hua ni Tohara na hayabatilishi Udhu,lakini pale itakapokua Maji Maji hayo ni Meupe na Masafi, kwani kama ikiwa yamechanganyika na Damu au Madhii basi Udhu Utakua umebatilika.

Na kama ikiwa Mwanamke hana uhakika juu ya asili ya Majimaji hayo ambayo ameyahisi baada ya kutia Udhu basi itambidi ajisafishe na kisha Atie Udhu Upya kabla ya kuingia kwenye Ibada ya Sala,na hii ni kutokana na kua huenda Maji maji hayo yakawani yenye kutoka ndani zaidi na hivyo kua si Tohara.

Naam..hivyo Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Rutubat Al Farj yaani Maji Maji ya kwenye Uke na Utohara wake.

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua ni Tohara na wala si Najis.Isipokua Wanafunzi wawili wa Imam Abu Hanifa wamesema kua Ni Najis.

Na anasema Imam Al Dasuqi Al Maliki kua Imam Al Qurtubi Al Maliki basi amesema kua: '**Wanazuoni Wanakubaliana kua Rutubat Al Farj kua ni Tohara, lakini Ibn Arafah basi yeye amesema kua kuna baadhi Wanasema kua ni Tohara, lakini Al Qurtubi yuko Sahih.'***(Hashiyat Al Dasuqi)*

Na akasema Imam wa Karne yetu Imam Mustafa Al Zarqa kua**: '*Rutubat Al Farj* ambayo ni Maji maji yanayomtoka Mwanamke kimaumbile katika mazingira ya kawaida hua si Najis Kulingana na Sharia za Kiislam na hivyo Haubatilishi Udhu.**

Kwani kama tukisema kua Yanabatilisha Udhu basi itakua kamwe haiwezekani kwa Mwanamke kudumu na Udhu wake, kwani hayamaliziki, na hivyo hii hua ni mbali na malengo ya Sharia ambayo ni kurahisisha mambo.'

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao kama tulivyosema kua wameyagawa Maji haya katika hali 3 kulingana na uasili wake aAmbazo ni *Rutubat Al Farj Al Kharija* yaani Maji maji ya Nje ya Mlango wa Uke au sehemu inayoonekana Pale Mwanamke anapochutama, *Rutubat Al Farj Al Dakhila* Maji Maji ya Mlangoni kuingilia. Ndani kwenye Uke ambapo Mawili yote haya hua ni Tohara lakini yakiwa hayakuchanganyika na Uchafu.

Na Rutubat Al Farj Ma wara Al Mihbal yaani Majimaji ya Ndani zaidi ya Uke karibu na Kizazi kua Si Tohara.

Ambapo kwa Wanaosema kua *Rutubat Al Farj* ni Tohara basi wanasimamia kwenye Uthibitisho wa kua:

1-Kila Kitu hua ni Tohara Kimaumbile hadi pale itakapothibitishwa kwa Si Tohara.

2-Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambayo amesema Ndani yake kua alikua akupamgusa Manii kutoka kwenye nguo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, na kutokana na Kua Mitume hawana Sifa ya Kuota kua Wanaingiliana Kimwili na Wanawake, basi hii inamaanisha kuaManii hayo yalikua yanayokana na Kuingiliana Kimwili kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Wake zake.

Hivyo kama Hukmu itakua *Rutubat Al Farj* ni Najis, basi hii itamaanisha kua hata Manii ya Mwanamke pia ni Najis kwa sababu yanatoka ndani ya Uke wake, hivyo uthibitisho wa kua Manii hayo yalipanguswa kwenye Nguo basi inamaanisha kua ni Tohara.

3-Hukmu ya Utohara wake unatokana na Kurahisisha mambo na kutoyafanya kua ni Magumu.

4-Kama yalivyo Majasho ambayo hua ni Tohara basi na *Rutubat Al Farj* hua ni Mithili ya Majasho ya Uke.

Ambapo wale wanaosema kua Rutbat Al Farj ni Najis basi wao wanasimamia kwenye Hadith zisemazo kua:

Amesema Abu Ayub kua amesema Kaab kua: Nilimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ya Rasul Allah Hivi Jee ni nini Hukmu ya Mtu atakaemuingilia Mkewe lakini akawa hakumwaga Manii?

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Anatakiwa ajisafishe sehemu Ya Mwili wake iliyomgusa Mwanamke kisha atie Udhu na Asali.'(Sahib Bukhari na Muslim)*

Na pia ile hadith isemayo kua: '**Amesema Zaid Ibn Khalid kua: Nilimuuliza Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* kua: Hivi Jee unafikiriaje kuhusiana na Mtu aliemuingilia Mke wake na kisha akawa hakumwaga Manii?'**

Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Anatakiwa ayie Udhu, kama wa Sala na pia ajikoshe Uume wake.'

Kwani mimi nimemsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam* akisema hivyo.

Zaid Ibn Khalid anasema kua:'Mimi nikawauliza Ali, Al Zubayr, Talha, na Ubbay Ibn Kaab ambapo nao wakaniamrisha hivyo.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo Hata hivyo Hadithi mbili hizi zimebatilishwa na ile hadith isemayo: '**Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Kama Mwanamme akikaa Baina ya Viungo vinne vya Mwili wa Mwanamke na kisha akajishindilia juu yake Mwanamke huyo Basi Hua Kuna Wajibu wa Kukoga Janaba hata kama Mwanamme huyo Hakumwaga Manii.'***(Sahih Muslim)*

Na hivyo hadith hii ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* imezibatilisha Hadith mbili za Abu Ayyub na Zaid Ibn Khalid, kwa kusema kua Yeyote atakaemuingilia Mkewe basi hua ni Wajibu kwake na Mke wake kujisafisha sehemu zao za Siri na Kukoga Janaba, na hii inathibitisha kua Rutubat Al Farj si Najis.

Kwani Amrisho la kukoga Janaba linatokana na kua Mtu anapoingiliana na Mkewe hua anatokwa na Madhii pia ambayo ni Najis hivyo Inambidi Kujitoharisha.

Na kisha wenye Kusema kua Rutubat Al Farj ni Najis wanasema kua kwa sababu Umajimaji huo huutoka kwenye Uke na hivyo sio sawa na Manii bali ni sawa na Madhii.

Naam, hivyo kama tulivyoona kuhusiana na Kutofautiana kwa Wanazuoni kuhusiana na Rutubat Al Farj yaani Maji Maji ya kwenye Uke na Utohara wake.Na hivyo basi tunahitimisha kwa kukumbushana kua Pale itakapokua Rutubat Al Farj ni yenye Rangi Nyeupe, Au yasiyokua na Rangi kama ya Maji ya Kawaida, au yana utelezi na mepesi na yana harufu kwa mbali na yasiyokua na Wingi basi Majimaji hayo ya Uke huhesabika kua ni Tohara au Masafi na hayabatilishi Udhu.

Lakini kama yakiwa yana rangi ya Manjano, Kijani, Pink,n.kNa yakawa yana Harufu kali na Mazito basi Maji Maji hayo yatahesabika kua ni Najis, na hivyo yatamuwajibisha Mwanamke alietokwa nayo kua ni Mwenye Kutenguka Udhu wake na hivyo atatakiwa ajitoharishe lakini si kwa kukoga Janaba bali kwa Kufanya Istinja.

Ambapo Istinja kwa Mwanamke hua ni Kukosha sehemu ya Uke inayoonekana wakati Mwanamke akiwa amechutama.Na hivyo hua kamwe haitakiwi Kutia Maji wala Sabuni ndani zaidi ya sehemu hizo.

Kwani anasema Al Alamaa Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyah Al Ansari Al Shafii kuhusiana na Istinja ya Mwanamke kua: ‘**Hua Inatosheleza kwa Mwanamke, iwe Mwanamke huyo ni Bikira au ni aliekwisha Olewa, kufanya Istinja kwa kukosha sehemu Zake za Siri za Mbele ambazo hua zinaonekana pale atakapokua amechutama***(Asna Matalib, Rawdha Talib)*

Kwani amesema pia Ummu Atiya Nusaybah Bint Kaab *Radhi Allahu Anha* kua:

كنا لا نعتدُّ بالصُّفرةِ والكُدرةِ بعدَ الغُسلِ شيئًا

Hakika sisi hatukua tukihesabu Unjano njano na uzito zito Unaotoka baada ya Kujitoharisha kua ni kitu chochote cha kukitilia Maanani*(Sahih Al Bukhari, Sunnan Abu Daud, Sunan Ibn Majah, Sunan An Nasai na Khulasat Al Ahkam - Imam An Nawawi)*

Ambapo hii ni hadith inayoonesha namna Masahaba wa kike walivyokua wakiishi katika wakati wa Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pamoja na wake zake R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambao walikua ni Walimu wao, kwa kusema kua walipokua wakiona Maji maji ya Njano Njano mazito kwenye nguo zao za ndani baada ya kumalizika kipindi cha hedhi basi walikua hawayatilii maanani.

Na hivyo hii haikuwazuia wao kufanya Ibada zao kama Kusali na kufunga bali walikua wakifanya Istinja unapowadia wakati wa Kusali na kisha hutia Udhu na kusali.

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MADII.

❖❖❖❖

Baada ya kuangalia kuhusiana na Manii na Madhii ya Wanaume na Wanawake na Hukmu zake Katika Uislam kulingana na Mitizamo ya Madhhab Tofauti na Maimamu tofauti na basi tumeweza kuona kua Maimamu wanakubaliana kuhusiana na Manii kua si Najis lakini yanapomtoka Mtu basi Humuwajibisha Kukoga Janaba, na hua hakuna Ulazima wa Kuifua Nguo Husika lakini inapedekezwa zaidi kuikosha pale itakapokua Una Uhakika kua Imeingia Manii tu.

Na tumeona kuhusiana na Makubaliano ya Wanazuoni kua Madhii kua Ni Najis na hivyo Yanapomtoka Mtu basi Hua anawajibika kuibadilisha Nguo husika kama imeingia Madhii na Kujikosha kila sehemu ya Mwili wake iliypingia Madhii na kisha Kutia Udhu Upya, kwani kwa kua Madhii ni Najis basi Udhu pia hubatilika.Hivyo umewadia wakati wa kukumbushana kuhusiana na Madii au Wadii na Hukmu yake kwa Wanawake na Wanaume.

Na anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kuhusiana na Madii kua: ‘**Madii hua Ni Maji Mazito,Meupe, Yenye kama wingu wingu ndani yake na ingawa hua yanafanana na Manii kiuzito lakini hutofautiana kwa upande wa wingu wingu wake na hua hayana Harufu**. **Madii hua yanatoka mara tu baada ya Mtu kumaliza kukojoa katika Tone la Mwisho la Mkojo,au pale Mtu anaponyanyua Kitu kizito. Na hua hayatoki mengi bali hua yanatoka Tone moja au mawili tu.**

Na Wanazuoni Wanakubaliana kua Hua hakuna Wajibu wa Kukoga Janaba pale inapokua Mtu ametokwa na Madhii au Madii.’*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na anasema Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Arafa Ad Dasuqi Al Maliki kua: ‘**Na fahamuni kua Wanawake pia hua wanatokwa na Madii baada ya Kumaliza kujisaidia haja Ndogo.’***(Hashiyah Al AdawiAl SharhAl Kharashi Al Maliki)*

Na amesema Al Allamaa Imam Hasan Al Shurunbulali Al Hanafi kua: '**Madii ni Maji meupe mazito yenye Uwingu wingu na hayana Harufu na Hutoka baada ya Kumalizika Kutoka Mkojo na pia Kabla ya Kutoka Mkojo.Madii ni miongoni mwa vitu ambavyo havimjwajibishi mtu kukoga Janaba vitakapomtoka, na Wanazuoni wanakubaliana kua Madhii na Madii hayamuwajibishi Mtu kukoga Janaba.**'*(Maraqi Al Falah Bi Imdad Al Fatah Sharh Nur Al Idda wa Najat Al Arwa)*

Ambapo anasema Imam Al Bayhaqi kua: '**Amesema Abu Nasr Umar Ibn Abd Al Aziz, kua amesema Ahmad Is-haq Ibn Shaybanah Al Baghdadi kua amesema Muadh Ibn Najdah kuamaesema Khalad Ibn Yahya kua amesema Malik Ibn Mughul kua amesema Zurah Abu Abd Rahman kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:**

الْمَنِيُّ وَالْوَدْيُ وَالْمَذْيُ، أَمَّا الْمَنِيُّ: فَهُوَ الَّذِي مِنْهُ الْغُسْلُ، وَأَمَّا الْوَدْيُ وَالْمَذْيُ فَقَالَ: اغْسِلْ ذَكَرَكَ أَوْ مَذَاكِيرَكَ وَتَوَضَّأْ وُضُوءَكَ لِلصَّلَاةِ

'Kuna, Manii,Madhii Na Madii, ama Manii ni Maji yanayowajibisha Kukoga Janaba, lakini kwa Madhii na Madii basi Jitohirishe Utupu wake wa Mbele na kisha Tia Udhu kama Unavyotia Udhu wa Sala.'*(Sunan Al Kubra Imam Al Bayhaq)*

Na Amesema Imam Ali Ibn Abd Allah Al Maliki Al Hindi kua:

عن مجاهد قال: بينا نحن جلوس أصحاب ابن عباس: عطاء وطاوس وعكرمة إذ جاء رجل وابن عباس قائم يصلي، فقال: هل من مفت؟ فقلت: سل. فقال: إني كلما بلت تبعه الماء الدافق، فقلنا: أي قال: إنا لله وإنا) الذي يكون منه الولد؟ قال: نعم، فقلنا: عليك الغسل فولى الرجل وهو يرجع وعجل ابن عباس في صلاته، فلما سلم قال: يا عكرمة، علي بالرجل، فأتاه به، ثم (إليه راجعون أقبل علينا فقال: أرأيتم ما أفتيتم به هذا الرجل عن كتاب الله؟ قلنا: لا. قال: فمن سنة رسول الله صلى الله عليه وسلم؟ قلنا: لا. قال: فعن أصحاب رسول الله صلى الله عليه وسلم؟ قلنا: لا. قال: فعمن؟ قلنا: عن رأينا. فقال: لذلك يقول رسول الله صلى الله عليه وسلم: فقيه واحد أشد على الشيطان من ألف عابد، ثم أقبل على الرجل، فقال: أرأيت إذا كان منك هل تجد شهوة في قلبك؟ قال: لا. قال: فهل تجد خدراً في جسدك؟ قال: لا. قال: إنما هو هذا بردة يجزئك منه الوضوء

Amesema Imam Mujahid Ibn Jabal kua: Wakati sisi tukiwa tumekaa na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Ataa, Tawus na Ikrimah basi alikuja Mtu wakati Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akiwa anasali na akatuuliza: 'Jee yuko yeyote miongoni mwenu anaeweza kutoa Fatwa?'

Imam Mujahid anasema kua: 'Mimi nikasema Uliza Suali lako.'

Mtu huyo akasema: 'Kila wakati mimi nikienda kukojoa basi hua kuna Maji fulani yanafuatia baada yake.'

Imam Mujahid anasema : 'Hivyo sisi sote tukamuuliza Jee ni yale yanayotoa Mtoto?'

Mtu huyo akasema: 'Naam!'

Imam Mujahid anaendelea kusema kua: 'Hivyo sisi tukamuambia Mtu huyo kua yakikutoka unatakiwa kukoga Janaba.'

Yule Mtu akasema: 'Inna Lillahi wa Inna Ilayhi Rajiun.'Na kisha akaondoka Na mara Ibn Abbas akamaliza Kusali Sala yake na kusema: 'Ikrimah! Hebu muite yule aliekuulizeni suali.'

Hivyo Ikrimah akanyanyuka na kumfuata yule mtu na akarudi nae, na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akatuuliza kwa kusema: 'Hebu niambieni Jee ile Fatwa mliyomtolea huyu Mtu mliitoa katika Kitabu cha Allah?'

Nasi tukasema: 'La!'

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Na Jee mliitoa katika Sunna za*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?.'

Nasi tukasema: 'La!'

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akauliza : 'Jee Mmeitoa kutoka kwa Mmoja kati ya miongoni mwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?'

Nasi tukasema: 'La!'

Abd Allah Ibn Abbs *Radhi Allahu Anhu* akaulia: 'Sasa Mmeitolea kutoka kwa Nani?'

Nasi tukasema: 'Hio ni kutokana na Mtizamo wetu.'

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Mnaona, hii ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: 'Mwanazuoni Mmoja hua ni Mgumu dhidi ya Shaytan kuliko Wafanyaji Ibada Elfu Moja.'

Na Kisha Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akamgeukia yule Mtu na Kumuuliza kwa kusema: 'Hebu niambie: Kama yanakutoka wewe Jee hua unakua na Matamanio ndani ya Moyo wako katika wakati huo?'

Mtu huyo akasema: 'La.'

Abd Allah Ibn Abbas akauliza: 'Jee yanapokutoka hua unakua na Msisimko kwenye Mwili wako?.'

Mtu huyo akasema: 'La!'

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema, 'Basi hayo ni Madii tu na hivyo Udhu tu utakua unakutosheleza.'*(Kanzu Al Amal)*

Na amesema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua:**‘Kuna makubaliano ya Wanazuoni kuhusiana na Madii kua yanabatilisha Udhu.’***(Al Mughni)*

Ambapo kwa upande mwengine basi Imam Ibn Qudamah al Hanbali Amemnukuu Imam Ibn Abd Al Barr Al Andalusi Al Maliki ambae amesema kua: **‘Amesema Imam Ibn Al Mundhiri kua: Kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni basi hua hakuna Ulazima wa Kutia Udhu pale yatakapomtoka Mtu Madii, bali Kujikosha tu kunatosheleza.’***(Al Dubyan Mawsuah Ahkami Al Taharat)*

Ambapo anasema Al Khatib Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shirbini Al Shafii kua: **‘Madii Ni Najis kutokana na kile kinachotoka kabla yake (Mkojo) na kulingana Na Makubaliano ya Wanazuoni.**’*(Al Mughni)*

Naam..amesema Imam Abu Al Husayb Al Imrani Al Yamani Al Shafii kua; **‘Madhii ni Najis kutokana na kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuamrisha Ali akoshe sehemu zake za Siri na pia Madii ni Najis kwa sababu yako sawa na Madhii.’***(Al Bayyan Fii Madhhab Al Shafii)*

Na pia amesema Imam Ibn Abi Shaybah kua amesema Imam Waki'i kua amesema Ikrimah Ibn Amar kua amesema Abd Rabih Ibn Musa kua amesema Mama yake kua: ‘**Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: ‘Manii yanawajibisha Kukoga Janaba, Madhii na Wadii yanawajibisha Kutia Udhu.’***(Musannaf Ibn Abi Shaybah)*

Naam tumeona kua Wanazuoni wanakubaliana kua Madii au Wadii ni yenye kutoka baada ya Kumalizika kutoka Mkojo na pia kabla yake kwa baadhi ya wakati hutoka pia baada ya mtu kubeba kitu kizito.

Na kua Madii ni Najis kutokana na kile kinachotoka kabla yake na yenye Kuwajibisha Kutia Udhu kwani yanabatilisha Udhu kwa yatakaemtoka wakati akiwa na Udhi iwe Mwanamme au Mwanammke.

Kwani amesema Imam Muhammad Ibn Ismail Al Bukhari kua:

قال ابن المنذر: وأما الودي ، فهو شيء يخرج من الذكر على أثر البول ، والوضوء يجب بخروج البول ، وليس يوجب بخروجه شيء إلا الوضوؤ وجب بخروج البول

‘**Amesema Imam Ibn Al Mundhiri kua: Al Wadiy hua ni Kitu kinachotoka katika Uume baada ya kumalizika Kutoka Haja ndogo.Hivyo Udhu hua unawajibika pale unapotoka mkojo, na hakuna Kinachowajibika katika kutolewa kwake isipokua Udhu unaotakiwa pale unapotoka Mkojo’***(Al Awsat)*

Ambapo tunapoiangalia kauli hii ya Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii basi tunaona kua mbali ya kua kuna Makubaliano ya Wanazuoni juu ya Kua Madii Ni Najis lakini hata hivyo kuna baadhi ya Wanazuoni wanaosema kua Madii peke yake hua si Najis, kwa mfano pale yanapomtoka Mtu atakapobeba kitu kizito.

Na hii ni kwa sababu kinachoyafanya Madii kua ni Najis hua ni kutoka kwake baada ya kutoka Mkojo ambao ni Najis. Kwa sababu hakuna uthibitisho ndani ya Qur'an wala Hadith Sahih usemao kua Wadii Ni Najis.

Na kutokana na kua hakuna uthibitisho huo basi basi kikanuni Madii hua ni Tohara, na kamwe haitoshelezi kua ni uthibitisho wa kua eti kwa sababu Madii yanatoka kwenye njia ya Mkojo na kwa Mkojo ni Najis basi nayo ni Najis. Kwani Hata Manii hua yanatoka kwenye Njia ya Mkojo lakini ni Tohara.

Hivyo kama ikiwa sababu ni kupitia kwenye njia ya mkojo baada ya mkojo basi Istinjaa (Kujisafisha kwa Maji) yake hua ni kutokana na Mkojo.

Ambapo hii ni hoja kati ya hoja za Kauli Moja kutoka kwa baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, kama Imam Al Mardawi Al Hanbali kama ilivyosemwa katika *Mawsuah Ahkami Toharat*.Na kwa upande wa Imam Al Kharashi katika *Sharh Mukhtasar Al Khalili* ambamo amesema kua: '**Ama kuhusiana na Madhii na Madii basi ni Tohara, ambapo baadhi wamenukuu Makubaliano ya Wanazuoni juu ya hilo.Na Imam Ibn Daqiq Al Id amenukuu juu ya hili kutoka kwa Imam Ahmad**.' *(Sharh Mukhtasar Al Khalili)*

Na bila ya shaka uthibitisho wa Aya au Hadith ambao hakuna ni wa kuhusiana na pale Madii yatakapotoka kabla ya kutoka Mkojo kaa kubena kitu kizito kama tulivyosema hapo Kabla.Kwani Uthibitisho wa Hadith uliopo ni wa Kutoka kwake baada ya Mkojo tu.

Ambapo Imam Zayn Ad Din Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Nujaym Al Misri Al Hanafi anajibu hoja kwa kusema kua: '**Jee ni nini manufaa ya kutakiwa kutia udhu kutokana na Madii yatokayo baada ya Mkojo?.'**

1-Faida ya Kwanza ni kwa wale wenye Matatizo ya Mkojo ambapo Kwao wao Mkojo hua hauwabatilishii Udhu lakini Madii yanawabatilishia Udhu. Ama kuhusiana na habari hii ya mkojo basi tutafafanu zaid kwenye Najis ya Mkojo.

2-Kama Mtu akitia Udhu baada ya kukojoa. **Kabla ya kutoka kwa Madii na kisha baadae yakatoka Madii basi Mtu huyo hutakiwa kutia Udhu tena.**

3-Madii hua pia ni Maji yanayotoka baada ya Kukoga, Baada ya Kuingiliana kimwili na pia baada ya kukojoa, na hua yana Mnato, na hivyo ndio ilivyoelezewa na katika Al Khazana na Al Tabyiin.

Hivyo Tatizo ni kua wale wenye kusema kua Madii ni Tohara basi wao wameangalia mtizamo wao katika hali ya kutoka baada ya kukojoa tu.

4-Wajibu wa Kutakiwa kutia Udhu baada ya Kukojoa hua haupingani na Wajibu wakutia Udhu baada kutokwa na Madii, na hivyo Udhu hua ni kwa ajili ya Vyote viwili.

Yaani hii inakua kama vile Mtu ambae ataapa kua hatotia Udhu tena baada ya kutokwa na Damu Puani, na kisha kisha akakojoa na akatia Udhu tena, ambapo hapa inakua hakutia Udhu kwa sababu ya kutoka na Damu Puani bali ametia kutokana na Kukojoa kwake, na Udhu huhitajika kwa vyote viwili.

Au kwa Mwanamke ambae atakula kiapo kutokoga Janaba baada ya Kutoka kwenye Hedhi lakini akaingiliwa na Mumewe na hivyo ikambidi akakoge Janaba kwa sababu ya Kuingiliana na Mumewe na wala si kwa sababu ya kumaliza Hedhi.

Ambapo katika haki zote mbili hizo Mtu hua amevunja Kiapo lakini kwa kua hakuvunja kwa nia ya kiapo bali amevunja kwa sababu nyengineyo iliyompelekea kukoga Janaba.' *(Al Bahr Raiq Sharh Kanz Al Daqaiq)*

ISTIBRA, NATR NA NADH KATIKA KUJITOHARISHA

❖❖❖❖

Ama tunapoangalia kuhusiana na namna ya kufanya *Istibra* yaani kujitoharisha baada ya kujisaidia haja ndogo kwa Wanaume ambapo kwa Wanawake hua ni *Istinjaa* kama tulivyoelezea hapo kabla basi tunaona kua *Istibra,* basi Hukmu za Sharia za Kiislam zimewekanjia au mfumo maalum ambao hua ni wenye kumhakikishia Mtu kujiondolea shaka na wasi wasi kutokana na kubakia na Madii baada ya kujisaidia na hivyo kufunga Mluango unaotumiwa na Shaytani katika kumtoa Ibn Adam husika katika hali ya utulivu katika ufanyaji wa Ibada zake.

Hivyo Wanazuoni wameweka wazihatua zinazotakiwa kuchukuliwa baada ya Mtu kujisaidia ambazo kwanza ni kufanya *Natr* na kisha kufanya *Nadh.* Ambapo kwa upande wa *Natr* hua ni kupitisha Kidole chini ya Uume baada ya Kujisaidia kuanzia mwanzo kuelekea kichwani ili kukamua na kuusukuma Mkojo wowote ule uliobakia au Madii ambayo yatakua yamebakia katika njia yake ndani ya Uume.

Na hii ni kutokana na uthibitisho wa Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: **'Wakati mmoja wenu atakapojisaidia basi na ajisafishe Dhakar yake mara Tatu.'***(Musnad Imam Ahmad, Marasil Abu Daud, Sunan Ibn Majah)*

Hivyo maana ya Natr hua inajumuisha Kusafisha Koo, Kusimama na Kuchutama tena na hii hua ni kulingana na Mila na Dasturi za Watu katika Jamii husika ambako nako kumepelekea Wanazuoi kutokukubaliana juu ya baadhi ya hatua hizi tatu tulizozitaja. Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Muhammad Alau Ad Din Al Haskafi Al Hanafi kua**: 'Hua ni Wajibu kujitoharisha kwa kutembea na kusafisha koo au kulala kwa upande wa kushoto, na hua inatofautiana kulingana na utofauti wa maumbile ya Watu husika'***(Durr Al Mukhtar)*

Na kwa upande wa Al Muhaqqiq Imam Ibn Aabidin Al Shami basi anasema kua: **'Baadi ya Wanazuoni wameelezea kwa kusema kua Natr hua ni Wajib, na kuna waliosema kua hua inabidina kuna waliosema kua inapendekezwa, kama walisvyosema baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab Imam Al Shafii. Hivyo hali yake ni kua kama ikiwa kua uhakika kua baada ua kufanya hivyo basi kuna kitu ambacho kitaonekana kua kimetoka basi bila ya shaka itakua inapendekezwa, na hu ani kuongeza chumvi katika kujitoharisha au katika kuelezea namna ya kujitoharisha kisha ikazugumziwa kuhusiana na vitu kama kutembea au kusafisha koo.'**

'Ama kuhusiana na kujitoharisha kwenyewe basi hua ni hadi pale Mtu atakapoijiridhisha ndani ya Moyo wake kua Najis yote imetoka. Na huo ndio Wajibu na ndio inayomaanisha kuhusiana na uwajibu wake. Hivyo amesema Al Shurunbulali kua: 'Mt hua anawajika kujisafisha hadi pale itakapokua hana matone ya Mkojo kwa kutoweka kwake na mtu husika akawa ni mwenye kuridhika ndani ya Moyo wake juu ya jambo hilo' na akasema kua: 'Nimetumia neno Wajib kwa sababu lenye nguvu kuliko kubidi kwa sababu kukosekana kwake hua ni kwenye kupelekea Mhusika kutoruhusika kuanza kutia Udhu hadi pale atakapokua na uhakika kua Njais yote imeondoka.' Na huu ndio Mtizamo Sahih, kua kama kiwa mtu ameihisi ndaiya Moyo wake kua ametoharika basi ndio ataruhusika Kutia udhu, na kila mt hua ni mwenye kujijua Moyoni mwake.' *(Raad Al Mukhtar)*

Ama kuhusiana na Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik basi amesema Imam Abu Walid Ibn Rushd Al Jadd Al Maliki kua: **'Ama kuhusiana na Kujitoharisha kutokana na Mkojo kwa kutumia njia ya kusimama na kisha kukaana kisha kukojoa, basi hua sis sahih kwani Rabia Ibn Abbi Abd Allah alikua na Homa kali san ana hivyo alikua akisimama katika sehemu ya karibu kila wakati, na kukojoa kila wakati, kisha akitia udhu na kurudi katika sehemu aliyokua amekaa, na mimi sikuwahi kumuona mtu ambae ni mwenye kutia udhu kwa haraka sana kama yeye, na juu ya hili imesemwa na Ibn Hurmuz ambae amesema kua Rabia ni Mwanafiqh Mahiri na amependezwa nae'** *(Al Bayan wa Al Tahsil)*

Na kasema Imam Shihab Ad Din Al Qarafi Al Maliki kua: '**Haitakikani kwa Mtu kusimama, kukaa na kusafisha koo yake bali ua antakiwa kufanya kile ambacho kitamtoshelza katika hali aliyokua nayo na anatakiwa ajitoharisha kwa kuitikisa Dhakar yake taratibu'** *(Al Dhakira)*

Na amesema Al Allamah Ibn Al Hajj Al Maliki kua: '**Mtu anatakiwa ajiangalie kujihakikishia katika wakati wa Istibra kulingana na Mazoea yake na Maumbile yake, kwani kuna mtu ambae anaweza kujitoharisha baada ya kujisaidia na kisha Mkojo kumalizika, wakati wengine huwabidi kusimama na kukaa na hii ni kulingana na utofauti wa hali yake ya kimaumbile, , chakula chake anachokula na utofauti wa wakati na mazingira, hali hubadilika kulingana na maabadiliko yake kimaumbile na kitabia na huaaa ni mwenye kujijua hali yake na hivyo kutakiwa kuchukua hatua stahiki kutokana na hali yake kama atakua na khofu ya Kusali bila ya kutoharika, na hivyo anatakiwa ajiangalie kulingana na hali yake na mazngira yake na chakula chake, kwani Mtu mzima hua si sawa na kijana, na anaekula Matikiti Hua si sawa na anaekula Jibini, na joto hua si sawa na baridi, na maesema Imam Abu Abd Allah Al Qurashi kua: 'Kama *Allah Subhanah wa Ta'ala* akimtakia Kheri Mja wake basi humjaalia kua na wepesi katika kujitoharisha kwake.' '***(Al Madkhal)***

Na Allaamah All Durir Al Maliki amesema kua: **'Msingi mkuu juu ya hili ni kuhakikisha kua Najsihio imekatika kutoka'***(Sharh Al Kabir)*

Na Imam Al Dasuqi amesema kua: '**Kama ikiwa Mtu atakua anafikiria kua Mkojo utakua umesita kwenye Dhakar yake basi anatakiwa aachane na kujitoharisha na asiendelee kuhesabia kuhusiana na wasi wasi juu ya kua labda kuna kitu kimebakia ndai ya Dhakar yake, na hivyo kama iiwa atakua hana uhakika kama kitu hcho kimetoka baada ya kujitoharisha, labda kama tone tu basi asilitilie maanani'***(Al Sharh Al Kabir)*

Ama kuhusiana na uande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi anasema Imam Al Haramayn kua: '**Mtu anatakiwa kufanya Istibra, hivyo anatakiwa kusubiri Matne ya Mkojo yamalizike na kisha asafishe Koo yake, na kila Mtu hua anajijua maumbile yake na kujisafisha ni kitu ambacho kimenukuliwa ambako hua ni kupitisha kidole chini ya Dhakar ili kusukuma mkojo uliobakia utoke, kama itakua umebakia**'*(Nihayat Al Matlab)*

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharafa An Nawawi amesema kua: **'Mtizamo unaopendekezwa Zaidi ni kua kuna kutofautiana kihali kwa kila mtu, hivyo kile kilichokusudiwa ni kua kama ikiwa mtu atakua anafikiria kua kuna kitu kimebakia katika njia ya mkojo na ana khofu kua huenda kikatoka nje basi baadhi ya watu hua na uwezo wa kujisafisha kutokana na hili kwa kujibinya mara moja. Wengine mara kadhaa, wengine kwa kujisafisha koo, wengine kwa kutembea hatua kadhaa wengine kwa kusubiri kidogo na wengine hua hawahitajii lolote kati ya haya.'**

‘Hivyo kila mtu anatakiwa asiwe ni mwenye kua na hali ya kufikiria sana juu ya hili kupita kiasi, ambapo As-habi Al Wujuh wetu wamesema kua: ‘Hali hii ya Kuitikisha Dhakari, Kusafisha Koo n.k hua inapendekezwa, hivyo kama ikiwa Mtu hakufaya hivyo lakini baada ya kukojoa na kisha akanawa basi Istinjaa yake hua sahih na Udhu wake hautobatilika na utakua kamili kwa sababu kikanuni kinachotakiwa ni kua kisitoke kitu baada yake, kwani anasema kua Kujitoharisha kwa Maji hua kunasitisha Mkojo, hivyo kujisafisha kwa Maji hua hakubatilishi tohara wala Udhu, isipokua pale Mtu atakapokua ana uhakika kua kuna kitu kimetoka’’*(Al Majmuu)***

Ama kuhusiana na Wanazuoni wa Madhhab wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi anasema Imam Abu Bakr Al Khallaal kua: ‘**Amsema Hanbal Ibn Is-haq Ibn Hanbal kua: ‘Nilimwambia mimi Abu Abd Allah, kua: ‘Nnahisi umaji maji baada ya Kutia Udhu’ ambapo nae akasema: ‘Usijiguse na Kujifuta hadi pale utakapohakikisha kua kuna kitu kimetoka nje, bali sita kwanza na achana nacho na wala usikitilie maanani kwa sababu hio itakua ni mnong’onezo wa Shaytan’’**’’*(Al Risala)* ambapo na Imam Adh Dhahabi amesema hivyo hivyo katika *Siyar Alam A Nubaala)*

Na akasema Imam Ibn Muflih Al Hanbali kua: **‘Inaonesha kua inapendekezwa kua ni mara tatu kwani baadhi ya Wanazuoni wetu wamesema kua mtu anatakiwa kusafisha Koo, na kuna waliosema kua atembee hatua kadhaa na Shaykh wetu Ahmad Ibn Hanbal amesema h ivyo pia. Ila amesema kua yote haya hua ni Bidaa na wala si Wajibu kulingana na makubaliano ya Wanazuoni’***(Muassasat Al Risalah)*

Ama kuhusiana na Nadh au Nadhuh basi hua ni Kurashia Maji kwenye Dhakar au kwenye Nguo ya Ndani kwenye sehemu ya Dhakar baada ya kufanya Istinjaa ili kuondoa Mawazo potofu ya wasiwasi ili kama mtu akiwaa ni mwenye kuhisi umaji maji basi asijali, ambapo kufanya hivyo hua si sehemu ya ukamilifu wa tohara. Ambapo Imam Ibn Majah na Imam Al Tirmidhi wamenukuu hadithi ya Abu Hurayrah *Radhi Allahuu Anhu* ambae amesema kua**: ‘Amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi w Salam* kua Jibril alikuja kwangu na kuniambia: ‘Muhammad katika wkati unapotia Udhu basi rashia Maji’’**

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Abd Razzaq basi nae amenukuu kwenye Musanaf yake kua: **‘Amesema Sufyan Ibn Al Hakam kua *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alikua akirashia majikwenye sehemu zake za Siri baada ya Kujisaidia haja ndogo au baada ya Kutia Udhu.’***(Musanaf Ibn Abd Razzaq, Musnad Imam Ahmad)*

Na imethibitishwa juu ya hili na Wanazuoni wa Hadith kama Imam Al Amir Al Saanani katika Al Tanwir amesema kua: ‘**Kilichomaanishwa katika kurashia Maji kaatia sehemu za Siri baada ya kutia udhu hu ani kuutokana na hikma ya kuondoa Wasi wasi**’*(Al Tanwir Al Jamii Al Saghir)*

Imam Ibn Majah, Imam Al Bayhaqi katika Sunan Al Kubra, ambapo Imam Al Tayyibi amesema kua: **‘Kurashia Maji hua kunamaanisha kurushia Maji kidogo kwenye sehemu za Siri baada ya Kutia Udhuu ili kuondoa wasiwasi, hivyo alijirashia maana yake alijirushia maji, na imesemwa kua *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alikua akifanya hivyo ili kuondoa wasiwasi wa kufikiria na *Allah Subhanah wa Ta’ala* alikua amemsitiri kutokana na Shaytan na amemjaalia Udhibiti wa Shaytan, lakini hata hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akifanya hivyo kwa ajili ya kuufundisha Umma wake, au alifanya hivyo kwa ajili ya kuzuia matone ya Mkojo yasitoke nje’***(Kashf Al Haqaiq Al Sunnan)*

Na amesema Imam Al Bayhaqi kua: **‘Amesema Said Ibn Jubayr kua kuna Mtu alikuja kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* na kusema Mimi hua nnahisi umaji maji pale ninaposimama kusali’, hivyo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akamwambia: ‘Jimwagie Gilasi ya Maji**

na hivyo ukihisi umaji maji basi jiambie kua ni kutokana nayo' na kisha baada ya hapo Mtu huyo akaondoka na hakurudi hadi baada ya mda mrefu kupita na kusema kua hali hio imemuondokea *(Sunan Al Kubra)*

Na amesema Imam Malik kua: '**Amesema Salt Ibn Zayyad kua: 'Nilimuuliza mimi Sulayman Ibn Yassir kuhusiana na Umaji maji anaouhisi nae akaniambia kua: 'Mwagia Maji chini ya kile kilichomo ndani Nguo zako za ndani na kisha pangusa''**'*(Malik Muwatta)*

Na imesemwa katika Al Mudawwanah ambacho ni kipande cha Fiqh ya Imam Malik kua: **'Amesema Ibn Wahb kua amesema Al Qasim Ibn Muhammad kuhusiana na Mtu mwenye kujioa kua ana umaji maji kua: 'Utakapomaliza kujitoharisha maji jirashie rashie Maji.''**

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Muammad Ibn Al Hasan Al Shaybani baada ya kunukuu hadith ya Salt Ibn Zayyad kua: '**Na hii ndio fatwa tunayoichukua kama ikiwa Mtu atakua ni mwenye kua na hali hii ya mara kwa mara inayosababishwa na Shaytan kumtia wasiwasi, na huu ndio pia mtizamo wa Imam Abu Hanifa'**

Na amesema Imam Al Sughadi Al Hanafi kua: **'Wanazuoni wetu wanachukulia kua hu anni Sunnah miongoni mwa Sunnah za Udhu kurashia maji pale inapokua Mtu anawasiwasi kama huo'***(Nutaf Al Fi Fatawi)*

Na Imam Badr Ad Din Ayn Al Hanafi: **'Ukisha tia Udhu basi Jirashie Maji, hua ina maana tofauti ikiwemo kujirushia maji kwenye nguo za ndani karibu na sehemu za Siri, ambapo hii hua ni yenye kuondosha wasiwasi kama ilivyotajwa kwenye Hadith'***(Sharh Abi Daud)*

Na Al Allamah Ibn Nujaym Al Hanafi: **'Kama ikiwa Shaytan anamtia wasi wasi Mtu kila wakati basi anatakiwa asitilie maanani bali anatakiwa alipuuzie jambo hilo na kisha ajirashie Maji kwenye sehemu zake za Siri kwenye Nguo zake hadi aondekewe na Shaka, na kisha aunasibishe Umaji maji huo kutokana Maji hayo hadi atakapokua na uhakika'***(Bahr Al Rahiq)*

Imam Al Baghawi Al Shafii kua: '**Na inasemwa kuhusiana na kujirashia Maji hua kunamaanisha kujimwagia Maji, kwa kujitoharisha, na pia hua inamaanisha kujirashia maji kwenye sehemu za Siri na kwenye Nguo za Ndani baada ya kujitoharisha kwa ajili ya kuondoa minong'ono ya Shaytani**'*(Sharh Al Sunnah)*

Na amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf an Nawawi kua: **'Wengi miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua: 'Kujirashia Maji kidogo katika sehemu za Siri baada Kujitoharisha hua ni kwa ajili ya kuondoa wasiwasi, na pia ndio imesemwa kua hua ni *Istinjaa* kwa Maji''***(Sharh Muslim)*

Ambapo anasema Al Hafidh Al Kabir Al Muharriri Imam Zayn Ad Din Abd Rahman Al Iraqi Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na kurashia Maji katika nguo baada ya Istinjaa, basi hua si kujitoharisha bali hua ni kuondoa hali ya wasiwasi, na hivyo atakapoona umaji maji basi na arashie rashie ili kuondoa wasi wasi na Allahu Aalam'***(Tarh Al Tadhrib)*

Na kwa upande wa Muwaffaq Ad Din Ibn Qudamah Al Hanbal kua: **'Inapendekezwa kurashia rashia Maji kwenye sehemu za Siri na kwenye Suruali kuondoa wasiwsi' na Imam Ahmad Ibn Hanbal aliulizwa kua: 'Jee ninatkiwa Kutia Udhu na kufanya Istibraa pale nnapohisi kua nna umaji maji?' Imam Ahmad Ibn Hanbal akasema: 'Utakapotia Udhu basi Jitiharishe kwa kuchukua Gao**

la Maji na kujirashia kwenye sehemu zako za Siri na wala usijali juu yake, kwani itaondoka Inshaa Allah' *(Al Mughni)*

Na Imam Al Buhuti Al Hanbal kua: **'Yeyote yule atakaekua anafikiria kua ametokwa na kitu, basi Imam Ahmad amesema kua hatakiwi kukitilia maanani kitu hicho hadi pale atakapokua na uhakik na hivyo aachane nacho, kwani hua ni kutokana na Shatyani na itaondoka Inshaa Allah'***(Sharh Al Muntaha Al Iradah)*

MANII NA RUTUBAT AL FARJ NI TOHARA; JEE INARUHUSIKA KUMEZWA?

❖❖❖❖

Baada ya kumalizana kuzungumzia kuhusiana na yanayobatilisha Udhu na Sala miongoni mwa yanayotoka katika sehemu za Mbele za Ibn Adam mbali ya Mkojo ambao badi hatujaangalia Juu yake.Lakini kwa upande wa Wanawake pia tumeangalia kuhusiana na aina tofauti za Damu na Hukmu zake. Lakini humpelekea yule yaliemtoka Kujitoharisha kwa kutawadha na kutia Udhu lakini bila kukoga.

Na tumeangalia kuhusiana na Manii kwa upande wa Wanaume na Wanawake, ambayo tulisema kua Manii ni Tohara ila yanamuwajiibisha kukoga Janaba yule yaliemtoka.

Na tukaangalia Madhii kwa upande wa Wanaume na Wanawake ambayo ni Najis lakini humpelekea yaliemtoka kujitoharisha kwa Kutawadha tu bila kukoga.Na tukamalizana na Madii kwa upande wa Wanaume na Wanawake ambayo pia hua ni Najis.

Na kisha tukazungumzia kuhusiana na Rutubat Al Farj yaani Maji Maji yanayomtoka Mwanamke kwenye Utupu wa Mbele.Ambao nao Hukumu yake ni kua kama Maji Maji hayo ni meupe na hayana harufu na yako kwenye Mlango wa Uke basi hua ni Tohara. Ambapo tunapozungumzia kuhusiana na Nje basi Wanazuoni wamesema kua ni sehemu ambayo hua inaonekana pale Mwanamke anapokua amechutama.

Na pia kama Maji Maji yakiwa ndani ya Mlango wa Uke katika sehemu inayokutana na Uume katika wakati wa kuingiliana kimwili basi hua pia ni Tohara. Ila kama yakiwa ni yenye kutoka ndani zaidi basi hua ni Najis.

Na kwa kua tulisema kua kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni kuhusiana na Manii Kua ni Tohara na Rutbat Al Farj pia ni Tohara na kila kilicho Tohara kua ni Halali kuliwa basi na tuangalie kuhusiana navyo vitu viwili hivi kama inaruhusika kutiwa mdomoni na kumezwa? Ama la? Kwa sababu hili ni suala ambalo wanajiuliza wengi sana miongoni mwa Vijana wa karne yetu.

Hivyo kwanza kwa upande wa Manii basi bila ya Shaka kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik kwa kua wao wamesema kua Manii si Tohara basi kwa upande wao pia hua hairuhusiki Kumeza au Kula Manii ya Ibn Adam.

Ambapo kwa upande mwengine basi tunaona kua kuna wanaosema kua: Suali la Kumeza Manii hua linahitajia kwanza kupata Ushauri wa Wataalamu wa Afya ambao kama Watathibitisha kua hayana Madhara basi hata kwa upande wa Dini itakua inakirihisha Kuyameza au Kuyala, kwa sababu ya

Maumbile yake kama zilivyosema Aya zilizozungumzia Maumbile ya Ibn Adam Na kama ikithibitishwa kua yana Madhara basi bila ya Shaka itakua Haram kuyameza.

Na bila ya shaka jambo hili limezungumziwa na Wanazuoni waliotangulia pia kama Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakkariyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi ambae amesema kua:'**Kuhusiana na Suali la kua Jee Inaruhusika Kumeza Manii? Basi juu yake kuna Majibu Mawili, (la Kwanza ni kua Inaruhusika na la pili ni kua) kuna Mtizamo unaokubalika zaidi ambao ni kua Hairuhusiki kwa Sababu ya kua Kuna Wanaozuni wanaosema kua ni Najis. Na kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameharamisha Najis pale aliposema:**

﴿ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلۡأُمِّيَّ ٱلَّذِي يَجِدُونَهُۥ مَكۡتُوبًا عِندَهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَٱلۡإِنجِيلِ يَأۡمُرُهُم بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَىٰهُمۡ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنۡهُمۡ إِصۡرَهُمۡ وَٱلۡأَغۡلَٰلَ ٱلَّتِي كَانَتۡ عَلَيۡهِمۡ فَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ مَعَهُۥٓ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ﴾

Alla<u>dh</u>eena yattabiAAoona alrrasoola alnnabiyya al-ommiyya alla<u>dh</u>ee yajidoonahu maktooban AAindahum fee alttawr<u>a</u>ti waal-injeeli ya/muruhum bialmaAAroofi wayanh<u>a</u>hum AAani almunkari wayu<u>h</u>illu lahumu al<u>t</u>tayyib<u>a</u>ti wayu<u>h</u>arrimu AAalayhimu alkhab<u>a</u>-itha waya<u>d</u>aAAu AAanhum i<u>s</u>rahum waal-aghl<u>a</u>la allatee k<u>a</u>nat AAalayhim faalla<u>dh</u>eena <u>a</u>manoo bihi waAAazzaroohu wana<u>s</u>aroohu waittabaAAoo alnnoora alla<u>th</u>ee onzila maAAahu ol<u>a</u>-ika humu almufli<u>h</u>oona. *(Surat Al Aaraf 7:157)*

Tafsir: ***Wale ambao ni wenye kumufuata Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam asiejua kusoma wala kuandika, ambae wamemuona ameandikwa kwenye vitabu yao vya Tawrat na Injil.na anawaamrisha Mema na kuwakataza Maovu na anaewahalalishia Vizuri na vitamu vya Halaili na amewaharamishishia vibaya vya Haramu. Na amewapunguzia uzito mkubwa sana na vifungo vya minyororo walivyozuiliwa navyo. Hivyowale wenye kumuamini(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam) na wakamheshimu na kumnusuru na wakafata Nuru ya Qur'an aliyoshushiwa, basi hao ndio waliofuzu.'***(Al Majmuu)*

Hivyo mbali yakua haipendekezwi kuyamezwa Manii lakini hata hivyo tunapozungumzia kuhusiana na Kupapasana, Kusuguana, kunyonyana na kubusiana sehemu za Siri basi hili ni moja kati ya mambo ambayo ni muhimu sana tunapozungumzia kuhusiana na mahusiano ya kimapenzi baina ya Mume na Mke hususan pale wanapotaka kuridhishana kimwili, kwani amaesema Jabir Ibn Abd *Allah Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **amekataza kuingiliana kimwili baina ya Mume na Mke kabla ya Kuchezeana,**'*(Tibb An Nabawi)*

Na amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amaesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam k*ua Asitokee mmoja wenu kuingiliana na Mke wake kama wanavyoigiliana Wanyama.' Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaulizwa: 'Ndio vipi hivyo ya *Rasul Allah?' Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kwa kubusianana na kuambiana maneno matamu.'***(Ihya Ulum Ad Din, Musnad Al Firdaws)*

Na imesemwa kwenye Fatawa Al Hindiyyah kua: **'Imam Abu Yusuf alimuuliza Imam Abu Hanifa kwa kusema: 'Jee unasema kuhusiana na Mume ambae atauchezea Uke wa Mke wake na Mke ambae atauchezea Uume wa Mume wake ili upate kusimama?' Imam Abu Hanifa akasema: 'Hamna Tataizo, na nna uhakika kua Mtu atalipwa Thawabu kutokana kufanya hivyo.''**

Na Imam Muhammad Amin Ibn Amr Ibn Abd Al Aziz Ibn Aabidin Al Shaami Al Hanafi amesema kua: **'Inaruhusika kwa Mume kumtia vidole Mke wake kwenye Uke wake ili Mwanammke huyo aweze kufikia kileleni mwa matamanio ya kuingiliana na pia inaruusika kwa Mke kuuchezea na kuusugua Uume wa Mume wake pia.'***(Radd Al Mukhtar)*

Na imesemwa katika Fatawa Al Hindiyyah kua: **'Ama kuhusiana na kama ikiwa Mke atauingiza Uume wa Mume wake Mdomoni mwake, basi kwa upande mmoja kuna Wanazuoni wanaosema kua hii hua haipendekezwi nakuna wanaosema kua Inaruhusika na haikirihishi.'***(Fatawa Rahimiyyah na pia katika Fatawa Hindiyyahna Fatawa Rashidiyya*)

Na amesema Imam Muhammad Ibn Ahmad Al Mayara amesema kua:

يجوز لكل من الزوجين النظر لفرج الآخر ولحسه بلسانه وكذلك السيد مع امته وقيل بكراهة ذلك

'**Inaruhusuika kwa kila mwenza (baina ya Mume na Mke) kuramba kwa ulimi wake sehemu za siri za mwenzake, na pia inaruhusika kwa Mtu na Mtumwa wake, na imesemwa kua inakirihisha'***(Al-Durr Al-Thamin Sharh Al-Murshid Al-Mu'in)*

Na vile vile amesema Shaykh Al Qaradawi kua: **'Wanazuoni Wanaruhusu hilo yaani kwa Mume kumnyonya Mke wake Na Mke kumnyonya Mume na hakuna ubaya juu yake. Isipokua kama ikiwa katika kunyonya huko kutapelekea kumwagika kwa Manii basi hii itakua ni Makruh, lakini hakuna Uthibitisho wa wazi juu yake.'**

Na Akasema Mufti Ali Gomaa Al Masri Al Shafii kua: **'Kunyonyana, kubusiana, kurambana kwa sehemu za Siri za Mume na Mke hua kunaruhusika kisharia pale itakapokua inapatikana Starehe katika Maingiliano ya Kimwili na hivyo kumpelekea mtu kutojishughulisha na mambo ya haram kwake kutoka nje ya ndoa yake. Na inabidi Kila Muislm awe anajua akilini mwake kua, maingilian ya kimwili baina ya Mume na Mke hua ni kwa ajili ya kuridhishana Kimwili ambapo kunatakiwa kuridhishana kwa njia za kihalali, na wala isichukuliwe kua kama kinywaji au chakula kama wanavyofanya watu wa Magharibi.'**

Ambapo aliulizwa Shaykh Abdul Wahhab Ibn Nasir Al Turairy wa Saudia suali lifuatalo: **'Mimi ni Mwanamke ambae nimeolewa kwa mda wa mwaka mmoja na Mume wangu anataka nimnyonye Uume wake, na animwagie Manii mwilini mwangu. Jee nini hukmu yake Jambo hili?'**

Shaykh Abdul Wahhab Ibn Nasir Al Turairy akajibu kwa kusema: **'Kitendo hicho hua kinakubalika baina ya Mume na Mke, kwani kuna mambo mawili tu ambayo yamekatazwa ambayo ni Kuingiliana katika wakati wa Hedhi au Nifasi na Kuingiliana kwa njia ya Nyuma.**

Hivyo nakushauri mimi kumkubalia Mume wako na kumridhisha ili apate kua Msafi na asiwe ni mwenye kutafuta njia ya kujistarehesha kwa kutafuta Mwanamke mwengine zaidi yake. Namuomba Allah Akuongoze.

Na kuhusiana na Kunyonya Uume basi hua inaruhusika baina ya Mume na Mke, na Kukumwagia Manii pia mwilini mwako inakubalika kwa sababu Manii ni Tohara. Na Mwanammke kuutia Mdomoni Uume wa Mwanamme, na Mwanamke kuweka Midomo yake kwenye Uke wa Mwanamke knaruhusika kwani hua ni sehemu ya kustareheshana baina ya Mume na Mke.'

Hivyo tunapoangalia kuhusiana na vitabu vya Fiqh basi tunaona kua Wanazuoni wametofautiana juu yake kwani kuna wanaosema kua kufanya hivyo hua inaruhusika na kuna wanaosema kua haipendekezwi, ambapo mitizamo hii hua haitegemeani na hali ya kua ni ukinyaa na si kinyaa kwa

kulingana na mtizamo wa watu tofauti bali ni kutokana na kua kufanya hivyo hua si kulingana na utamadini wa Kiislam.

Na kwa tunapoangalia kwa upande wa*Rutubat Al Farj* au Unyevunyevu wa Uke na hukmu zake, kama Kunyonyana na Kubusiana maeneo hayo baina ya Mke na Mume ama la basi jawabu la suali hili hua ni lenye kuruhusika kwa sababu malengo ya ndoa ni kupeana utulivu na kurudhishana baina ya Mume na Mke, pale itakapokua hakuna kuvunja sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ndani yake kwa kusababishiana madhara ya kimwili au kiafya, na hakuna kuingiliana kinyume cha maumbile na kuingiliana katika wakati ambao Mwanamke yuko katika hedhi, kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿أُحِلَّ لَكُمْ لَيْلَةَ ٱلصِّيَامِ ٱلرَّفَثُ إِلَىٰ نِسَآئِكُمْ هُنَّ لِبَاسٌ لَّكُمْ وَأَنْتُمْ لِبَاسٌ لَّهُنَّ عَلِمَ ٱللَّهُ أَنَّكُمْ كُنتُمْ تَخْتَانُونَ أَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَيْكُمْ وَعَفَا عَنْكُمْ فَٱلآنَ بَاشِرُوهُنَّ وَٱبْتَغُواْ مَا كَتَبَ ٱللَّهُ لَكُمْ وَكُلُواْ وَٱشْرَبُواْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ ٱلْخَيْطُ ٱلأَبْيَضُ مِنَ ٱلْخَيْطِ ٱلأَسْوَدِ مِنَ ٱلْفَجْرِ ثُمَّ أَتِمُّواْ ٱلصِّيَامَ إِلَى ٱلَّيْلِ وَلاَ تُبَاشِرُوهُنَّ وَأَنْتُمْ عَاكِفُونَ فِي ٱلْمَسَاجِدِ تِلْكَ حُدُودُ ٱللَّهِ فَلاَ تَقْرَبُوهَا كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ آيَاتِهِ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ﴾

Ohilla lakum laylata alssiyami alrrafathu ila nisa-ikum hunna libasun lakum waantum libasun lahunna AAalima Allahu annakum kuntum takhtanoona anfusakum fataba AAalaykum waAAafa AAankum faal-ana bashiroohunna waibtaghoo ma kataba Allahu lakum wakuloo waishraboo hatta yatabayyana lakumu alkhaytu al-abyadhu mina alkhayti al-aswadi mina alfajri thumma atimmoo alssiyama ila allayli wala tubashiroohunna waantum AAakifoona fee almasajidi tilka hudoodu Allahi fala taqrabooha kadhalika yubayyinu Allahu ayatihi lilnnasi laAAallahum yattaqoona *(Al Baqara 2:187)*

*Tafsir:**Imeahalalishwa juu yenu kua na maingiliano ya kimwili na Wake zenu katika Usiku wa Siku za Funga, kwani wao (Wake zenu)ni vazi kwa ajili yenu na nyie ni Vazi kwa ajili yao pia. Kwani Allah ni mwenye kujua mlikua mkijidanganya nafsi zenu, hivyo amekugeukiani na kukusameheni. Hivyo sasa hivi kuweni na mahusiano ya kungiliana kimwili nao na mtafute kile ambacho Allah amekiamrisha kwa ajili yenu, na kuleni na kunyweni hadi utakapodhihirika weupe wa muangaza wa Alfajiri utakaotofautisha weusi wa kiza cha usiku, kisha timizeni Funga zenu hadi utakapoingia Usiku, na wala msiwe na mahusiano ya kuingilana kimwili nao katika wakati mkiwa kwenye Itikafu Miskitini. Hii ndio mipaka ya Allah aliyoiweka hivy msiwakaribie. Kadhalika hivyo ndivyo anavyobainisha Allah Aya zake kwa Watu ili wawe Wacha Mungu.***

Ambapo aya imetumia neno *Rafatha* lenye kumaanisha Kuingiliana Kimwili, Kufanya mapenzi, Kulala na kufanya Mapenzi, Kufanya mambo ambayo hayawezekani kufanywa mbele za watu, Kufanya mambo kwa siri bila ya kuoneana haya baina ya Mwanamme na Mwanamke. Na piaikatumia Neno Libas ambalo humaanisha Nguo, Ngao, Vazi, Gamba au Gome ambalo hua na kazi ya Kumlinda na kumhifadhi Mtu kutokana na athari za nje ya mwili wake, na kumsababishia Mtu kuridhikana kua na utulivu kutokana na kuhifadhika kwake na pia kumpendezesha Mtu husika, Hivyo aya inadhihirisha kua Wanaume ni Mavazi kwa ajili ya Wanawake, na Wanawake ni Mavazi kwa ajili ya Wanaume katika Kupatiana utulivu, kuhifadhiana, kuridhishana, na kupendezeshana.

Na kisha akasema tena *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿نِسَآؤُكُمْ حَرْثٌ لَّكُمْ فَأْتُواْ حَرْثَكُمْ أَنَّىٰ شِئْتُمْ وَقَدِّمُواْ لأَنْفُسِكُمْ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱعْلَمُوٓاْ أَنَّكُمْ مُّلاَقُوهُ وَبَشِّرِ ٱلْمُؤْمِنِينَ﴾

Nisaokum harthun lakum fa/too harthakum anna shi/tum waqaddimoo li-anfusikum waittaqoo Allaha waiAAlamoo annakum mulaqoohu wabashshiri almu/mineena *(Al Baqara 2:223)*

Tafsir: ***Wake zenu ni Mashamba yenu, hivyo yaendeeni Mashamba yenu mtakavyo na tangulizeni (kufanya mema) kwa ajili ya Nafsi zenu na muogopeni Allah, na jueni kua mtakutana nae na Wabashirie (habari Njema) Waumini.***

Tunapoiangalia aya hii katika kutumia kwake neno *Harthun* basi tunona kua inamaanisha kua Mume hua ni Mkulima, Mke hua ni Shamba. Manii Hua ni Mbegu na Mtoto anaepatikana kutokana na mchanganyiko wa Makadirio na Majaaliwa ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Jitihada za Mkulima katika kulihudumia Shamba lake hua ndio Matunda yanayotokana na Shamba hilo.

Hivyo basi Wanazuoni wanasema kua Kiislamu inaruhusika kwa Mume na Mke Kubusiana, Kunyonyana, Kurambana sehemu za Siri kwa ajili ya kustareheshana na kuridhishana kimapenzi baina ya Mume na Mke lakini bila ya kuvuka mipaka iliyowekwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na haya yamedhihirishwa wazi kwenye Vitabu kadhaa vya Fiqh kulingana na mitizamo ya Wanazuoni wengi sana akiwemo Imam Abu Muhammad 'Ata' Ibn Abi Rabah Al Makki Al Qurayshi alizaliwa katika mwaka 25 Al Hijra, ambapo anasema Imam Muhammad Ibn Abd Allah Ad Dibaj kua: '**Hakika mimi sijawahi kuona Mufti aliekua ni bora zaid ya Ataa Ibn Abi Rabah**' kwani Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua anaposomesha Darsa basi Darsa yake ilikua ni yenye kua na Nuru ya *Dhikr Allah* na anapoulizwa suali na akatoa Fatwa basi hua anatoa kwa ufafanuzi wa kina kwani alikua na Ilm kubwa ya Fiqh, Quran, Tafsir na Hadith.

Imam Ataa Ibn Abi Rabah alikua ni mwenye Ilm kubwa sana ya Ibada ya Hija, kiasi ya kua katika wakati wa Uhai wake ambao ulikua ni wakati wa Utawala wa Banu Ummayah, basi kila inapofika Ibada ya Hija mji wa Makkah hua ni wenye kutangaziwa kua: **'Hairuhusiki kwa Mtu yeyote kutoa Fatwa kuhusiana na Ibada ya Hija isipokua Imam Ataa Ibn Abi Rabah, na kama sio yeye basi anaeruhusika baada yake ni Abd Ibn Abi Najih**'

Hivyo anasema Imam Ataa Ibn Abi Rabah kua: '**Inaruhusika kwa Mume kumbusu Mke wake katika sehemu zake za Siri, lakini kabla yakuingiliana nae, kwani hua inakua makruh kumbusu sehemu hizo baada ya kuingiliana nae.**'(*Al Insaaf, Kitab An-Nikah)*

Na akasema Imam Al Qurtubi Al Maliki kua:**'Qadhi Ibn Arabi Al Maliki amesema kua Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Mume kuziangalia sehemu za Siri za Mke wake**. **Na mtizamo mmoja wao ni wanaosema kua Inaruhusika kama kufanya hivyo kutamsababishia kupata raha na hua ni bora zaidi**. **Na amesema Imam Ibn Sabagh kua Inaruhusika kwa Mume hata kuchezea Uke wa Mkewe kwa Ulimi wake.'***(Jamii Ahkami Al Qur'an)*

Na imesemwa pia katika Mawahib Al Jalil Sharh Mukhtasar Al Khalil kua: '**Aliambiwa Imam Ibn Sabagh kua Kuna Watu wamesema kua Haipendekezwi**: '**Imam Al Sabagh akasema: Wanaosema haipendekezwi ni kwa sababu ya Mtizamo wao Kiafya lakini si Kiutaalam,kwa sababu hakuna**

tatizo lolote Kuuangalia Uke na Kuuchezea kwa Ulimi pia.'(*Mawahib Al Jalil Sharh Mukhtasar Al Khalil)*

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi haya yamezungumziwa pia kwenye *Al Majmuu cha Imam An Nawawi, Tuhfah Al Muhtaj, Fat-h Al Muin, Ianat Al Talibin, Hashiyat Al Bujaraimi, Kashaf Al Qina, Al Insaaf na katika Al Mughni.*Ambapo tunapoangalia vitabu hivi basi tunaona kua Wanazuoni wa Fiqh wameruhusu matumizi ya Mwili Mzima wa Mume kwa Mke na Mwili Mzima wa Mke kwa Mume kwa ajili ya kujitosheleza Kimatamanio lakini bila ya kuvuka Mipaka ya Kimaumbile na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ambapo mbali ya Kua Wanazuoni hua Hawaruhusu kuguswa kwa Najis bila ya dharurah inayokubalika Kisharia, ambapo tunapozungumzia kuhusiana na yale yanayotokea katika wakati wa kitendo cha Mapenzi baina ya Mume na Mke hua ni sababu inayoruhusika, ambapo hata hivyo Kama tulivyoona kuhusiana na Manii basi hukmu yake ni Tohara, Rutubat Al Farj pia ni Tohara.

Na tunapozungumzia kuhusiana na Madhii na Wadii basi Sharia zimeruhusu kwa Mume na Mke kuchezeana ili kuridhishana hata kama yatatoka Manii, au Madhii, au Madii na hata Rutubat Al Farj.

Na mbali ya kua Inaruhusiwa Kula Vitu vyote vya Halali lakini hua haipendekezwi kumeza vitu ambavyo mbali ya kua Tohara lakini hua pia vinahesabiwa kua ni Kinyaa.

Ambapo amesema Imam Ahmad Zayn Ad Din Al Malibari Al Shafii kua:

يَجُوزُ لِلزَّوْجِ كُلُّ تُمَتَّعُ مِنْهَا بِمَا سِوَى حَلَقَةِ دُبُرِهَا وَلَوْ بِمَصِّ بَظْرِهِ

'Inaruhusika kwa Mume kujistarehesha Kwa Kila sehemu ya Mwili wake, Hata kama kumnyonya Kinembe chake.isipokua sehemu ya Haja Kubwa.' *(Fat'h Al Muin)*

Na akasema Imam Al Damyati Al Shafii kua:**'Inaruhusika kwa Mume kustarehe na kila sehemu ya Mwili wa Mke wake wote, au wa Suriyyah wake wote, au wa Mtumwa wake wa Kike wote isipokua Sehemu zake Utupu wa Nyuma, ambapo Imekatazwa kumuingilia kwani kufanya hua ni Liwat**. **Na inaruhusika kustarehe nae hata kwa Kunyonya kinembe.'***(Ianat At Talibin)*

Na akasema Imam Mansur Ibn Yunus Al Buhuti Al Hanbali kua: **'Inaruhusika kubusu sehemu za Siri za mbele wa Mke Kabla ya Kumuingilia ila inakirihisha kufanya hivyo baada ya kumuingilia.'**

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Imam Ibn Ya'la Al Hanbali katika Kashf Al Qina.Na ndio Mtizamo wa Imam Ibn Aqil na Imam Al Mardawi ambao wote ni Wanazuoni wa Madhhab ya Ima. Hanbal na wametumia neno *Umsus Badhr* ambalo kwa kiarabu cha asili humaanisha Kunyonya Kinembe.

Ambapo amesema Mujaddid Ad Din Ibn Hajar AlAsqalani Al Shafii kua: **'Badhr (بَظْر) ni Kipande cha nyama ambacho hua juu ya Uke kinachobakia baada ya Kutahiriwa'**

Na amesema Imam Al Kharashi kuhusiana na ayah hii kua: **'Maana yake maneno ya ayah hii ni kua Jistarehesheni naokatika kila sehemu isipokua Njia ya Haja kubwa'***(Mukhtasar Al Khalil)*

Na Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafi nae amesema pia kua: '**Ama kuhusiana na kujistarehesha nao wake kwa kila kitu hua inaruhusika na hamnatatizo lolote isipokua ni kua iwe bila ya kumuingilia baina ya Matako yake'***(Al Umm)*

Na akasema Imam Zakarriyah Al Ansari kua: **'Mume hua ana haki ya kujistarehesha kwa mkewe kwa kila namnaanavyotaka hata baina ya Matako isipokua kwenye Njia ya Haja kubwa, ambayo ni sehemu iliyokatazwa kumuingilia kutokana na hadith isemayo kua: 'Allah si mwenye kuona haya kusema ukweli, hivyo msiwakaribie Wanawake kwenye njia zao za Nyuma' ambayo ni hadith iliyonukuliwa na Imam Al Shafii na kuthibitishwa nae usahihi wake'***(Asna Matalib)*

Na amesema Imam Zayn Ad Din Ibn Ibrahim Ibn Nujaym kua: '**Kila kilichokatazwa kina uharamu wa eneo la mipaka yake isipokua katika hali moja tu ambayo sikuona Mtu yeyote ambae amependelea kuweka mipaka juu yake, ambacho ni njia ya haja kubwa ya Mke, ambayo imekatazwa lakini kuna udhihirisho wa wazi kua inaruhusika kujistarehesha na mipaka ya eneo lake ambayo ni baina ya Matako.'***(Kitab Ashbah wa al Nazir)*

Anasema Al Khatib Al Shirbin kua: '**Na Kustareheshana (kwa kupapasana, kubusiana, n.k) katika njia ya haja kubwa inaruhusika lakini bila ya kuingiliana.'(***Tuhfah Al Habib)*

Na Imam Ad Dasuqi amesema kua: **'Inaruhusika Kuchezea sehemu ya Nje ya Haja Kubwa' yaani hata kwa kuweka Uume juu yake kwani kile kilichozugumziwa juu ya sehem a nje yake hua ni sehemu ya Tundu yake na maana hata Imam Al Barzili akasema kua: 'Nadhi kuruhusika kwake kunatokana na uhalali wa Mwili wote wa Mwanamke, kwa kua hakuna Hadith iliyoelezea kuhusiana na sehemu ya nje yake kama vile iliyokua katika sehemu ya Ndani yake.'** *(Hashiyah Al Dasuqi)*

Na imesemwa kwenye Al Mawsuah Al Fiqhiyyah kua: **'Wengi miongoni mwa Wanazuoni wanasimamiA kwenye mtizamo wa kua inaruhusika kwa Mume kujistarehesha na sehemu ya Nje ya Haja Kubwa ya Mke wake kwa sharti la kua iwe bila ya kumuingilia, nah ii ni kwa sababu sehemu hio hua ni sawa na sehemu n yenginezo za mwili wake ambazo zimeruhusiwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* isipokua kuingia ndani yake.'**(*Mawsuah Al Fiqhiyyah al Quwaitiyyah)*

Na akasema Imam Al Maradawi Al Hanbali kua: '**Imam Ibn Jawzi amesema kua Wanazuoni hawapendekezi kumuingilia Mwanamke kwa kupitia baina ya Matako yake kwa sababu ya kua itapelekea kumuingilia kwa njia ya Nyuma.'**

Na amesema Al Shahid Imam Muhammad Said Ramadhan Al Buti kua: **'Haki baina ya Mume na Mke hua haiishi kwenye mipaka ya kuingiliana kimwili tu, bali kulingana na kile ambacho Qur'an imekitaja kua ni Starehe kwa ujumla, ambapo hii inamaanisha kua kila Mtu baina ya Mke na Mume Anayohaki ya kustareheka na mwenza wake kwa kadiri anavyotaka, iwe katika kuingiliana ama kwa njia nyengineyo, ambapo ndani yake hapa hayaingii mambo yafuatayo tu:**

1-Kuingiliana katka wakati wa Hedhi.

2-Kuingiliana Kwa njia ya Nyuma.

3-Kufanyiana yale ambayo yatasababisha madhara baina ya Mume na Mke kama ilivyothibitishwa na Madaktari.'

Hivyo tukiachana na mambo matatu haya basi hukmu na kanuni za Kisharia zinabakia kuweka wazi kua mengine yote yaliyobakia yanaruhusika. Hivyo matamanio yote ya kimaumbile ya kibinadam yanayotamaniwa na Ibn Adam kama kuingiliana na mengineyo yanayoendana

sambamba nayo hua ni haki ya kila mtu kwa mweza wake na hairuhusiki kumzuia mwenza au kumkatalia pale inapokua hakuna kisingizo kinachokubalika kisharia.

Ama kuhusiana na Matamamanio ya kistarehe baina ya Mwanamme na Mwanamke hua yanatofautiana sana baina ya wale wanaoona kua ni kinyaa na kuna wanaoona kua ni starehe wanayoitamani, na hivyo hua hua hakuna njia baina yao isipokua kukubaliana kwani hakuna mwenye haki ya kumlazimisha mwenzake juu ya kile anachokiona kua ni kinyaa.'

Na amesema Shaykh Muhammad Husein Issa wa Misri kua: **'Mume na Mke wanayohaki ya kustareheshanakwa kila namna, kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿نِسَآؤُكُمْ حَرْثٌ لَّكُمْ فَأْتُواْ حَرْثَكُمْ أَنَّىٰ شِئْتُمْ وَقَدِّمُواْ لأَنْفُسِكُمْ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱعْلَمُوٓاْ أَنَّكُمْ مُّلاَقُوهُ وَبَشِّرِ ٱلْمُؤْمِنِينَ﴾

Nisaokum harthun lakum fa/too harthakum anna shi/tum waqaddimoo li-anfusikum waittaqoo Allaha waiAAlamoo annakum mulaqoohu wabashshiri almu/mineena *(Al Baqara 2:223)*

Tafsir: ***Wake zenu ni Mashamba yenu, hivyo yaendeeni Mashamba yenu mtakavyo na tangulizeni (kufanya mema) kwa ajili ya Nafsi zenu na muogopeni Allah, na jueni kua mtakutana nae na Wabashirie (habari Njema) Waumini.***

Ambapo wamesema Wanazuoni kuhusiana na ayah hii kua inamaanisha kua stareheni na Wake zenu kwa kila namna, isipokua kwa ile namna ambayo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameikataza ambayo ni njia ya nyuma, yaani Mume hatakiwi kuingiza Uume wake kwenye njia ya Nyuma ya Mke, lakini anaruhusika kuchezea Matako na kila kilichomo baina ya Matako na sehemu nyengine zote isipokua kuingiza Uume kwenye njia ya Nyuma.

Ama kuhusiana na kustareheshana katika maeneo ya kuzunguka Njia ya nyuma na katika sehemu nyenginezo basi hua inaruhusika na Mume anatakiwa ajistareheshe kwa mkewe na Mke pia kwa Mumewe kwa kadri watakavyotaka.'

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- HAJA NDOGO NA KUBWA

❖❖❖❖

Kwani amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

مَرَّ النَّبِيُّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِقَبْرَيْنِ، فَقَالَ إِنَّهُمَا لَيُعَذَّبَانِ، وَمَا يُعَذَّبَانِ فِي كَبِيرٍ، أَمَّا أَحَدُهُمَا فَكَانَ لاَ يَسْتَتِرُ مِنَ البَوْلِ، وَأَمَّا الآخَرُ فَكَانَ يَمْشِي بِالنَّمِيمَةِ ثُمَّ أَخَذَ جَرِيدَةً رَطْبَةً، فَشَقَّهَا نِصْفَيْنِ، فَغَرَزَ فِي كُلِّ قَبْرٍ وَاحِدَةً، قَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ، لِمَ فَعَلْتَ هَذَا؟ قَالَلَعَلَّهُ يُخَفِّفُ عَنْهُمَا مَا لَمْ يَيْبَسَا

*'**Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam** **alipita baina ya Makaburi mawili, na akasema: 'Kwa hakika Watu wawili hawa wanaadhibiwa kwa Vitu ambavyo (waliviona kua) si Vikubwa.Kwani mmoja wao alikua si mwenye kujikinga kutokana na Cheche za Mkojo, na mwenzake alikua ni mwenye Kusambaza Uongo wa Kusingizia.' Na kasha akachukua Kuti bichi la Mtende na akalikata kati kati na kisha akakichomeka kila Kipande kwenye Kaburi Moja. Masahaba **Radhi Allahu Anhum** wakamuuliza: 'Ya Rasul Allah, Kwanini Umefanya hivyo?' **RasulAllah Salallahuu Alayhi wa Salam** akasema: 'Huenda ikawarahisishia hii wakati Majani yake hayajakauka'**(Sahih Bukhari na Muslim)*

Na pia kuna hadith isemayo:

حَدَّثَنَا أَبُو الْيَمَانِ، أَخْبَرَنَا شُعَيْبٌ، عَنِ الزُّهْرِيِّ، ح وَقَالَ اللَّيْثُ حَدَّثَنِي يُونُسُ، عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، أَخْبَرَنِي عُبَيْدُ اللَّهِ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُتْبَةَ، أَنَّ أَبَا هُرَيْرَةَ، أَخْبَرَهُ أَنَّ أَعْرَابِيًّا بَالَ فِي الْمَسْجِدِ، فَثَارَ إِلَيْهِ النَّاسُ لِيَقَعُوا بِهِ فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " دَعُوهُ، وَأَهْرِيقُوا عَلَى بَوْلِهِ ذَنُوبًا مِنْ مَاءٍ ـ أَوْ سَجْلاً مِنْ مَاءٍ ـ فَإِنَّمَا بُعِثْتُمْ مُيَسِّرِينَ، وَلَمْ تُبْعَثُوا مُعَسِّرِينَ

Amesema Abu Al Yaman kua amesema Shuaibu kua amesema Al Zuhriyi kua amesema Al Layth kua amesema Yunus, kua amesema Abu Shihab kua amesema Abdillah Ibn Abdillahi Ibn Utataybah kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:Kuna Bedui alikua akikojoa Msikitini, na hivyo Masahaba wakakimbilia kutaka Kumpiga Lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaamrisha Masahaba kumwachia hadi amalize haja yake kisha akawaamrisha kua Wachukue Maji Ndoo nzima waimwagie katika sehemu iliyokojolewa. Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Hakika Mmeletwa kwa ajili ya Kurahisisha mambo na wala si kwa ajili yaKuyafanya yawe Magumu.'*(Sahih Bukhari na Muslim)***

Naam.tumeanza na Hadith mbili hizi kwa sababu hizi ni miongoni mwa hadith maarufu ambazo ndio zenye kudhihirisha kua Mkojo ni Najis. Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: **'Ama kuhusiana na Mkojo basi hua uko wa aina Nne ambazo ni:**

1-Mkojo wa Ibn Adam ambae ameshakua Kiumri na hivyo ameshaachana na Kunyonya ziwa la Mama Yake.

2-Mkojo wa Mtoto Mchanga ambae hajaanza kula Kitu chochote isipokua ni mwenye kunyonya Ziwa la Mama yake tu.

3-Mkojo wa Mnyama ambae ni Halali Kuliwa.

4-Mkojo wa Mnyama ambae si halali Kuliwa.

Ambapo aina zote nne hizi za Mkojo hua ni Najis kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu na Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni.'***(Al Majmuu)***

Na akasema Imam Abu Al Husein Yahya Ibn Imran Al Yamani Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na Mkojo na Kinyesi cha Wanyama basi hua ni Najis kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu ya Al Shafii bila kuangalia kama Mnyama huyo halali kuliwa ama la.**

Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* na Imam Al Awzai. Na ndio Mtizamo wa Wanazuoni wetu wa Tawi la Baghdad.' *(Al Bayan Fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Naam..Imam Al Imran amesema hivi hapa kuhusiana na Tawi la Madhhab ya Imam Al Shafii la Baghdad kwa sababu ya kulingana Historia ya Imam Al Shafii Mwenyewe ambae kabla hajahamia Misri basi aliwacha Wanafunzi katika Ardhi ya Baghdad akiwemo Imam Ahmad Ibn Hanbal, na wengineo.

Na pia historia ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi Wanazuoni wake walikua wamegawika katika sehemu mbili, ambazo ni sehemu ya Wanazuoni wa Mashariki yaani Baghdad, Iran na Khurasan, na kisha kuna Wanazuoni wa Mashariki ambao ni wa Misri, Yemen na Syria.

Na hali ilibakia hivi hadi alipokuja *Hujjat ul Islami* Imam Abu Hamid Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali ambae ndie akaziunganisha Pande mbili hizi na hivyo chini yake yeye ikawa kuna Tawi Moja tu.

Na hii ni mada nyengine ambayo ni ndefu na nzuri sana na tumeshaizungumzia Miaka 10 Nyuma na Nimeiandikia Kitabu. Hivyo kwa atakaeitaka basi na atafute kitabu cha Ijtihad na Taqlid Historia ya Uislam, Maimamu na Madhhab yao katika Uislam cha Al Mustakshif Abu Manal Danah ambacho kinapatikana bure mtandaoni.

Kisha Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: **'Ama kuhusiana na Mkojo wa Mtu Mzima ambae ameshaacha Kunyonya yaani aina ya kwanza basi kuna Makubaliani juu ya Wanazuoni juu ya kua ni Najis. Na Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri ndie alienukuu Makubaliano hayo.**

Na mbali ya Makubaliano hayo ya Wanazuoni lakini pia Kuna urhibitisho wa Hadith tuliyoitaja Ama kuhusiana na Mkojo wa Mtoto Mdogo ambae hajaanza kula chochote isipokua Maziwa ya Mama yake ambao ni wa aina ya pili basi pia Ni Najis kulingana na sisi Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii na pia kulingana na Wanazuoni wote kwa Ujumla bila kuwepo mwenye kupinga.

Na Al Abdari na Mwandishi wa Al Bayan yaani Imam Al Imran wamenukuu Mtizamo kutoka kwa Abu Daud kua Mkojo wa Mtoto Mchanga ni Tohara. **Ambapo Mtizamo wetu sisi ni wenye kutokana na Hadith na pia Makisio ya Qiyas kulingana na Mkojo wa Mtu mzima**. **Na vile vile imethibitishwa na Hadith kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoharisha Nguo yake kutokana na Mkojo wa Mtoto mchanga kwa kuimwagia Maji, hivyo kama si Najis basi asingeimwagia Maji Nguo.**

Ama kuhusiana na aina ya Tatu 3 ya Wanyama wanaoliwa basi Mkojo wao na Kinyesi chao pia ni Najis. **Na hii ni kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, ya Imam Abu Hanifa, Abu Yusuf na wengineo.**

Ambapo Imam Ataa, Imam Al Nakhai, Imam Al Zuhri Imam Malik, Imam Sufyan Al Thawry, Dhafar na Ahmad *Radhi Allahu Anhum* basi wao wanasema kua Mkojo na Kinyesi cha Wanyama Wanaoliwa hua si Najis bali ni Tohara.Ambapo Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Al Imran muandishi wa Al Bayyan ambae ni Miongoni mwa Wanazuoni wetu.

Na vilevile Imam Al Rafii amenukuu Mtizamo huu pia kutoka kwa Imam Al Istakhri na Imam Al Ruwayni. Ambao nao wameuchukua Mtizamo huo kutoka kwa Imamu wa Maimamu Anu Bakr Muhammad Ibn Is-haq Ibn Khuzaymah Al Shafii ambae pia ni miongoni mwa Wanazuoni wetu, ambae yeye ameutoa kwenye Hadith Sahih na kutoa udhibitisho wake.Lakini Hata Hivyo Mtizamo Unaojulikana sana na kukubalika zaidi katika Madhhab yetu ni Wa Uhakika kua Mkojo na Kinyesi cha Wanyama wanaoliwa ni Haram.

Ama kwa upande wa Imam Al Layth Ibn Saad na Imam Muhammad Ibn Hasan basi wao wana Mtizamo wa kua Mkojo wa Wanyama wanaoliwa ni Tohara, lakini si Kinyesi chao, wakati Imam Abu Hanifa anasema kua Kinyesi cha Njiwa ni Tohara.

Ama kuhusiana na Mkojo wa Mnyama asieliwa yaani wa aina ya 4 basi ni Najis na hii ni Kulingana na Mtizamo wa Imam Al Shafii, Imam Malok, Imam Abu Hanifa, na Wanazuoni wote bila ya kupingana. Ingawa Imam Al Qafal Al Shashi Al Marwazi na wengineo wamenukuu mtizamo kutoka kwa Imam Ibrahim An Nakhai ambae amesema kua Mkojo wa Mnyama asieliwa kua ni Halali na Si Najis.

Lakini Mimi siamini Mtizamo huo kua umenukuliwa kutoka kwake, na hata kama utakua ni wa kwake basi hauwezi kukubalika.Na kwa upande wa Imam Ibm Hazim amesema katika Al Mahalla kua amesema Imam Abu Daud kua Mkojo na Kinyesi cha Viumbe wote hua ni Tohara isipokua Mkojo na Kinyesi cha Ibn Adam ambavyo ndio Najis,na hii Sio Sahih.'*(Al Majmuu Sharh Mujadhdhab)***

Baada ya Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi baada ya kuainisha Mitizamo tofauti ya Wanazuoni kuhusiana na Mkojo wa Wanyama wanaoliwa kua ni Tohara ama la, basi anaendelea kutupa vithibitisho vya Ushahidi waliotoa na kuusimamia wale Wanaosema kua Mkojo huo ni Tohara kwa kusema kua:

حَدَّثَنَا مُوسَى بْنُ إِسْمَاعِيلَ، حَدَّثَنَا هَمَّامٌ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ أَنَسٍ ـ رضى الله عنه ـ أَنَّ نَاسًا، اجْتَوَوْا فِي الْمَدِينَةِ فَأَمَرَهُمُ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم أَنْ يَلْحَقُوا بِرَاعِيهِ ـ يَعْنِي الإِبِلَ ـ فَيَشْرَبُوا مِنْ أَلْبَانِهَا وَأَبْوَالِهَا، فَلَحِقُوا بِرَاعِيهِ فَشَرِبُوا مِنْ أَلْبَانِهَا وَأَبْوَالِهَا، حَتَّى صَلَحَتْ أَبْدَانُهُمْ فَقَتَلُوا الرَّاعِيَ وَسَاقُوا الإِبِلَ، فَبَلَغَ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم فَبَعَثَ فِي طَلَبِهِمْ، فَجِيءَ بِهِمْ فَقَطَعَ أَيْدِيَهُمْ وَأَرْجُلَهُمْ، وَسَمَرَ أَعْيُنَهُمْ. قَالَ قَتَادَةُ فَحَدَّثَنِي مُحَمَّدُ بْنُ سِيرِينَ أَنَّ ذَلِكَ كَانَ قَبْلَ أَنْ تَنْزِلَ الْحُدُودُ

Ni Hadith isemayo kua: Amesema Musa Ibn Ismail kua amesema Hammam kua amesema Qatadah kua amesema Anas *Radhi Allahu Anhu* kua:

Hali ya Hewa ya Madina haikuwakubali baadhi ya Watu (wa Uraynah), Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawaamrisha wamfuate Mchungaji wa Wanyama wa Ngamia wake, na kisha wamwambie kua awapatie Maziwa na Mkojo wa Ngamia kisha wanywe kama Dawa

Hivyo Watu hao wakafuata Mchungaji huyo Wakapewa na Wakanywa Maziwa na pamoja na Mkojo wa Ngamia hao na wakapona. Na kisha Wakamuua Mchungaji na Kuwaiba Ngamia hao

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **alipopata Habari hio basi akawatuma Watu wakawafukizie, na Wakakamatwa na Kurudishwa kwenye Mji wa Madina na Wakakatwa Mikono yao na wakapigwa Mihuri ya Moto Juu ya Macho yao.'***(Sahih Bukhari na Muslim)*

Hivyo Imam An Nawawi anasema kua:**'Wafuasi wa Madhhab ya Malik na Ahmad Ibn Hanbal waliitumia Hadith hii kua ni uthibitisho wa kua Mkojo na Kinyesi cha Wanyama wanaoliwa kua si Najis.**

Lakini Wanazuoni wetu wa Madhhab ya Imam Al Shafii pamoja na Wanazuoni wengineo wanasema kua Mkojo na Kinyesi cha Wanyama Wanaoliwa ni Najis. Na hivyo ingawa Mkojo wao ni Najis lakini inaruhusika Kuutumia kwa ajili ya Kujitibu kama inavyoruhusika kutumia Najis nyengine zote kama Dawa inapobidi isipokua Vilevi,na ndio maana Watu hawa wakaruhusiwa Kunywa Mkojo wa Ngamia.

Ama kuhusiana na Wale Wanaosema Kua Mkojo wa Wanyama wanaoruhusika Kuliwa kua ni Najis basi wao Wanasimamia kwenye Uthibitisho tulioutoa hapo kablan(Wa kua Imeruhusika kwa sababu ni Dawa) na pia hapo hapo Imam Al Shafii ametoa Ushahidi kwa kusema kua Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua;

ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلْأُمِّيَّ ٱلَّذِى يَجِدُونَهُۥ مَكْتُوبًا عِندَهُمْ فِى ٱلتَّوْرَىٰةِ وَٱلْإِنجِيلِ يَأْمُرُهُم بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَىٰهُمْ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ ٱلْخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَٱلْأَغْلَٰلَ ٱلَّتِى كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۚ فَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُوا۟ ٱلنُّورَ ٱلَّذِىٓ أُنزِلَ مَعَهُۥٓ ۙ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ

Alla<u>dh</u>eena yattabiAAoona alrrasoola alnnabiyya al-ommiyya alla<u>th</u>ee yajidoonahu maktooban AAindahum fee alttawr<u>a</u>ti waal-injeeli ya/muruhum bialmaAAroofi wayanh<u>a</u>hum AAani almunkari wayu<u>h</u>illu lahumu al<u>t</u>tayyib<u>a</u>ti wayu<u>h</u>arrimu AAalayhimu alkhab<u>a</u>-itha waya<u>d</u>aAAu AAanhum i<u>s</u>rahum waal-aghl<u>a</u>la allatee k<u>a</u>nat AAalayhim faalla<u>dh</u>eena <u>a</u>manoo bihi waAAazzaroohu wana<u>s</u>aroohu waittabaAAoo alnnoora alla<u>th</u>ee onzila maAAahu ol<u>a</u>-ika humu almufli<u>h</u>oona*(Surat Al Araf 7:157)***

Tafsir: ***Wale ambao ni wenye kumufuata Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam asiejua kusoma wala kuandika, ambae wamemuona ameandikwa kwenye vitabu yao vya Tawrat na Injil.na anawaamrisha Mema na kuwakataza Maovu na anaewahalalishia Vizuri na vitamu vya Halaili na amewaharamishishia vibaya vya Haramu. Na amewapunguzia uzito mkubwa sana na vifungo vya minyororo walivyozuiliwa navyo. Hivyowale wenye kumuamini(Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam) na wakamheshimu na kumnusuru na wakafata Nuru ya Qur'an aliyoshushiwa, basi hao ndio waliofuzu.'***(*Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab*)

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye amesema kua: **'Kinyesi na Mkojo wa Wanyama Wanaoliwa hua Ni Tohara ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam An Nakhai, Sufyan Ath Thawry na Malik.'***(Al Mughni)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MKOJO WA NGAMIA

❖❖❖❖

Naam..hivyo Kulingana Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Mkojo wa Wanyama wa aina zote hua ni Najis iwe Mnyama huyo ni wa Kufuga Ama la, ambapo kwa upande wa Ngamia basi Ingawa Mkojo wake hua ni Najis kulingana na Mtizako wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Abu Hanifa lakini hua inakubalika kunywa kutokana na kua ni Dawa kama tulivyofafanua kulingana na Vithibitisho vya Hadith na pia vya Kisayansi.

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Malik basi wao wamesema kua Mkojo wa Ngamia si Najis.

Na kwa upande mwengine basi amesema Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Sahl Ahu Bakr Al Sarakhasi Al Hanafi kua:

'Kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Hanifa basi hua hairuhusiki Kunywa Mkojo wa Mnyama ambae Nyama yake ni Halali kuliwa na hii ni kutokana. Na hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua : Hakika *Allah Subhanah wa Ta'ala* hakuweka Tiba kwenye kile ambacho amekuharamishieni.'

Imam Al Sarkhasi anaendelea kusema kua: '**Lakini kwa Upande wa Imam Muhammad Ash Shayban basi yeye amesema kua inaruhusika kunywa Mkojo wa Mnyama anaeliwa kwa ajili ya Dawa au jambo jengine, na hii ni kwa sababu Kwake yeye Imam Ash Shaybani Mkojo wa Mnyama anaeliwa ni Tohara Ama kwa upande wa Imam Abu Yusuf basi yeye amesema kua Itaruhusika Kunywa Mkojo wa Mnyama anaeliwa lakini kwa ajili ya kujitibu tu basi, na hii ni kulingana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipowaruhusu watu wa Uraynah kunywa Mkojo wa Ngamia kama Dawa.'***(Al Mabsut)***

Hivyo Mtizamo wa Imam Abu Yusuf Al Hanafi ambae ni Mwanafuni wa Imam Abu Hanifa ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam An Nawawi kua: **'Wanazuoni wetu wanakubaliana kua inakubalika Kutumia Najis na aina za Vilevi kwa ajili ya Matibabu, na huo Ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni pia.'***(Al Majmuu)*

Na akasema tena Imam An Nawawi kua: '**Hukmu ya kukubalika Kutumia Mkojo wa Ngamia kwa ajili ya Tiba ni kutokana na Amrisho la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa watu wa Urainah kama ilivyosema Hadith.'***(Al Majmuu)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi akasema kwenye *Rawdhah Talibin* kua: **'Kuna Mtizamo usemao kua hairuhusiki Kutumia Najis kama Mkojo wa Ngamia hata kwa ajii ya Tiba lakini Mtizamo huo ni Dhaifu hauna nguvu.***'(Rawdha Talibin)*

Na hii ni kutokana na Kanuni ya Fiqh isemayo kua:

***Al Dharuuraat Tabyih Al Mahtuurat* yaani Dharurah Huruhusu Kilichoharam kua Halali.**

Na bila ya shaka Ili Kilichoharamu kihalalike kwenye Dharurah ya Kiafya basi Wanazuoni wameweka Masharti yafuatayo:

1-Kitu Hicho kilichoharamishwa Lazima Kijulikane kua pia hua ni Dawa

2-Kama ikiwa Mtu hana Uhakika nacho basi anatakiaa atafute Ushauri wa Mtu mwenye Ilm ya Tiba

3-Inatosheleza Kuomba Ushauri wa Mtaalamu mmoja wa Ilm ya Tiba ambae ni Muislam*(Imam Al Baghawi, Imam An Nawawi Al Majmuu)*

Na akasema Imam Badr Ad Din Al Ayni Al Hanafi kua: **'Kutafuta Tiba kutokana na Vitu vilivyoharamishwa kama Dawa hua inaruhusika pale inapokua Mtu ana uhakika wa kua Kitu hicho Kitamponesha. Kwani hii hua inakua ni sawa na Kuruhusika Kula Nyama ya Mnyama aliekufa pale Mtu anapokua katika Hali mbaya sana ya Njaa na hakuna chakula, na pia Kunywa Pombe pale Mtu anapokua anatakakufa kwa Njaa na Maji hakuna.***'(Umdat Al Qari)*

Na Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali amesema kua: **'Mkojo na Kinyesi cha Mnyama ambae Nyama yake Inaliwa hua ni Tohara. Kwani Amesema Imam Malik kua Wanazuoni hawauhesabu Mkojo na Kinyesi cha Mnyama anaeliwa kua ni Najis. Na Imam Ibn Al Mundhiri amesema kua: 'Kila Mtu niliesoma kwake Miongoni mwa watu wenye Ilm basi wanakubaliana kua Inaruhusika Kusali kwenye Banda la Kondoo, isipokua Al Shafii tu ambae amesema kua Inabidi Banda hilo liwe tohara kutokana na Mikojo na Kinyesi cha Kondoo hao.**'

Na Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* alikutikana akisali katika sehemu ambayo kulikua na Kinyesi cha Kondoo, na akaambiwa Kwanini usije ukasali hapa? Ambapo nae akauliza: 'Hapa nilipona hapo kotoe ni sawasawa'.

Na *Rasul Allah Salallahu A'layhi wa Salam* na Masahaba zake *Radhi Allahu Anhum* walikua walikua hawana sehemu maalum za Kusalia kama kwenye Mazulia au Misala na walikua wakisali juu ya mchanga ardhini, na Wanyama kama Kondoo walikua hawaachani na Mikojo yao n vinyesi vyao, na hivyo hii inamaanihsa kua Walikua wakigusana navyo katika nyakati za Ibada za Sala zao, kwani ni mchanganyiko wa kawaida kwa Mnyama ambae Nyama yake inaliwa, basi Kiyesi chake hua niTohara na kama Maziwa yake na kinyesi cha Ndege kwa wanaokubaliana na hilo.

Kwani kamaingekua si Tohara basi Majani ambayo Ng'ombe hua wanayakanyaga yangekua pia si Tohara, kwa sababu hua hayaachani na Mkojo wao bali yanashikamana na Mkojo wao, hivyo baadhi ya Wanyama hawa wagekua ni Najis na baadhiy yao wangekua Tohara, hivyo ikiwa katika hali kama hii basi Wanyama wote hao wangekua katika Hukmu ya kua ni Najis*(Al Mughni)*

Na tunapoangalia vithibitisho vya wanaosema kua hairuhusiki kutumia vilivyo haram kwa ajili ya matibabu tunaona kua ni pamoja na Hadith isemayo:

عَنْ أَبِي الدَّرْدَاءِ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «إِنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ الدَّاءَ وَالدَّوَاءَ وَجَعَلَ لِكُلِّ دَاءٍ دَوَاءً فَتَدَاوُوا وَلَا تداوَوْا بحرامٍ» . رَوَاهُ أَبُو دَاوُد

Amesema Abu Darda *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* Kua: Hakika ya Allah ameshusha maradhi yote na tiba yake na amechagua tiba kwa kila aina ya maradhi, hivyo jitibuni kwa kutumia Dawa lakini mtumie chochote kile ambacho ni haram.'*(Sunan Abu Daud)*

Na amesema Abu Bakr Ibn Abi Shaybah, kua

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، وَهِشَامُ بْنُ عَمَّارٍ، قَالاَ حَدَّثَنَا سُفْيَانُ بْنُ عُيَيْنَةَ، عَنْ زِيَادِ بْنِ عِلاَقَةَ، عَنْ أُسَامَةَ بْنِ شَرِيكٍ، قَالَ شَهِدْتُ الأَعْرَابَ يَسْأَلُونَ النَّبِيَّ ـ صلى الله عليه وسلم ـ أَعَلَيْنَا حَرَجٌ فِي كَذَا أَعَلَيْنَا حَرَجٌ فِي كَذَا فَقَالَ لَهُمْ " عِبَادَ اللَّهِ وَضَعَ اللَّهُ الْحَرَجَ إِلاَّ مَنِ اقْتَرَضَ مِنْ عِرْضِ أَخِيهِ شَيْئًا فَذَاكَ الَّذِي حَرَجٌ " . فَقَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ هَلْ عَلَيْنَا جُنَاحٌ أَنْ نَتَدَاوَى قَالَ " تَدَاوَوْا عِبَادَ اللَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ سُبْحَانَهُ لَمْ يَضَعْ دَاءً إِلاَّ وَضَعَ مَعَهُ شِفَاءً إِلاَّ الْهَرَمَ " . قَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ مَا خَيْرُ مَا أُعْطِيَ الْعَبْدُ قَالَ " خُلُقٌ حَسَنٌ "

Amesema Hisham Ibn Amar kua amesema Sufyan Ibn Unaynah kua amesema Ziyad Ibn Ilaqat kua amesema Usamah Ibn Shariqah kua Nimemshuhudia mimi Bedui mmoja akimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: 'Jee kuna dhara yoyote katika kadha na kadhaa? Na kadhaa wa kadhaa?' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Enyi Waja hakika ya Allah amekijaalia dhara kile cha Mtu chenye kumvunjia heshima ya ndugu yake, yaanikile chenye kua ni Dhambi'

Watu wakasema: 'Ya Rasul Allah, Hivi jee kuna kosa lolote kama hatukutafuta Tiba?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Tafuteni Tiba enyi waja wa Allah, kwani Allah hakuumba Maradhi yeyote isipokua ameumba na Tiba yake, isipokua Uzee' Watu wakauliaza: Ya Rasul Allah Hivi Jee ni kitu gani ambacho ni bora kwa Mtu kujaaliwa?'**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Ni Tabia Njema'(Musannaf Ibn Abi Shayba)*

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: ***'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza Kutumia Dawa zisizokua Tohara'** *(Sunan Abu Dawud)*

Na amesema tena Imam Abu Daud kua:

حَدَّثَنَا مُسْلِمُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ، حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، عَنْ سِمَاكٍ، عَنْ عَلْقَمَةَ بْنِ وَائِلٍ، عَنْ أَبِيهِ، ذَكَرَ طَارِقَ بْنَ سُوَيْدٍ أَوْ سُوَيْدَ بْنَ طَارِقٍ سَأَلَ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم عَنِ الْخَمْرِ فَنَهَاهُ ثُمَّ سَأَلَهُ فَنَهَاهُ فَقَالَ لَهُ يَا نَبِيَّ اللَّهِ إِنَّهَا دَوَاءٌ . قَالَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم " لاَ وَلَكِنَّهَا دَاءٌ "

Amesema Muslim Ibn Ibrahim kua amesema Shu'bat kua amesema Simak kua amesema Alqamah Ibn Waili kua amesema Baba yake kua amesema Tariq Ibn Suwayd au Suwayd Ibn Tariq kua alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Pombe, lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Aliikataza, hivyo akamuuliza tena, na akamkataza tena, hivyo akamuuliza kwa kusema: 'Ya Rasul Allah, Hua ni Dawa' *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La Ni Maradhi'*(Sunan Abu Dawud, no: 3869)*

Na amesema Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* kua: ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua:**

إِنَّ اللَّهَ لم يجعَلْ شفاءَكُم فيما حرَّمَ عليكُم

Hakika ya Allah hakuweka Tiba kwa ajili yenu kwenye vile vilivyoharamu. *(Sahih Ibn Hibban)*

Ambapo kuhusiana na wale wanaosema kua inaruhusika basi wanasimamia kwenya vithibitisho vifuatavyo: **Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ ٱلْمَيْتَةَ وَٱلدَّمَ وَلَحْمَ ٱلْخِنزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ بِهِۦ لِغَيْرِ ٱللَّهِ فَمَنِ ٱضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَلَآ إِثْمَ عَلَيْهِ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

Innama harrama AAalaykumu almaytata waalddama walahma alkhinzeeri wama ohilla bihi lighayri Allahi famani idturra ghayra baghin wala AAadin fala ithma AAalayhi inna Allaha ghafoorun raheemun*(Surat Al Baqara 2:173)*

Tafsir: ***Amekukatazeni Nyinyi Maiti, na Damu na Nyama ya Nguruwe na kile ambacho hakikuchinjwa* Kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Lakini Yeyoye yule atakaekua na Dharura Na Akawa Hana Njia Nyengine isipokua kuasi (Kwa kula hivyo vilivyotajwa) Wala si kutokana na Matamanio basi kwa Hakika Mola wako Ni mwingi wa Usamehevu na ni Mwingi wa Huruma.**

Na kuna hadith isemayo:

حَدَّثَنِي مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ، حَدَّثَنَا غُنْدَرٌ، حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، سَمِعْتُ قَتَادَةَ، عَنْ أَنَسٍ، رَخَّصَ أَوْ رُخِّصَ لِحِكَّةٍ بِهِمَا.

Amesema Muhamamd Ibn Bashr kua amesema Ghun-dar kua amesema Shu'bat kua amesema Anas kua amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua**: 'Wameruhusiwa (Zubayr na Abd Rahman *Radhi Allah Anhum*) kuvaa Hariri (Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*) kutokana na tatizo la Kuwashwa kwao'** *(Sahih al-Bukhari)*

Ambapo hadithi hii inatuonesha kuruhusika kuvaliwa kwa hariri kutokana na tatizo la kuwashwa kwa ngozi za Masahaba hawa wawili ambao ni Zubayr na Abd Rahman *Radhi Allahu Anhum* mbali ya kua imekatazwa kwa Wanaume katika hadith isemayo:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ سَلاَمٍ، قَالَ: أَخْبَرَنَا أَبُو الأَحْوَصِ، عَنْ أَشْعَثَ، عَنْ مُعَاوِيَةَ بْنِ سُوَيْدٍ، عَنِ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ قَالَ: أَمَرَنَا رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم بِسَبْعٍ، وَنَهَانَا عَنْ سَبْعٍ: أَمَرَنَا بِعِيَادَةِ الْمَرِيضِ، وَاتِّبَاعِ الْجَنَائِزِ، وَتَشْمِيتِ الْعَاطِسِ، وَإِبْرَارِ الْمُقْسِمِ، وَنَصْرِ الْمَظْلُومِ، وَإِفْشَاءِ السَّلاَمِ، وَإِجَابَةِ الدَّاعِي. وَنَهَانَا عَنْ: خَوَاتِيمِ الذَّهَبِ، وَعَنْ آنِيَةِ الْفِضَّةِ، وَعَنِ الْمَيَاثِرِ، وَالْقَسِّيَّةِ، وَالإِسْتَبْرَقِ، وَالدِّيبَاجِ، وَالْحَرِيرِ.

Amesema Muhamamd Ibn Salami kua amesema Abu Al Khawas kua amesema Ash-A'ath kua amesema Mawwiyah Ibn Suwayd kua amesema Baraa Ibn Azib *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Tumearishwa sisi na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Mambo Saba ambayo ni:

Kuwatembelea Wagonjwa, Kujumuika na msafara wa Jeneza, Kuwaombea Rehma watakopiga Chafya, Kutimiza Ahadi na Nadhiri, Kuwanusuru wanaodhulumiwa, Kurudisha Salamu, na kukubalia Mialiko. Na Ametukataza Kuvaa Pete za Dhahabu, Kutumia Vyombo vya Fedha, Kutumia Masoji ya Hariri nyekundu, Kuvaa nguo zenye mchanganyio wa Hariri, Kuvaa Nguo zilizojaa jaa, Kuvaa mapambo ya Hariri na kuvaa Hariri asilia. '*(Adab Al Mufrad)*

Na inagawa hadithi hii imezungumzia kukatazwa kwa Wanaume kuvaa Dhahabu lakini pia kuna Hadith isemayo kua:

عن عبد الرحمن بن طرفة، أن جده عرفجة بن سعد قطع أنفه يوم الكلاب، فاتخذ أنفا من ورق، فأنتن عليه، فأمره النبي صلى الله عليه وسلم فاتخذ أنفا من ذهب.

'Amesema Abd Rahman Ibn Tarfa kua Babu yake ambae ni Urfajah Ibn Sad alikatwa Pua katika Vita vvya Al Kilab, na hivyo akachonga Pua ya Fedha na kujibandika lakini ikaanza kunuka hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuamrisha achonge Pua ya Dhahabu.'*(Sunnan Abu Daud)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MKOJO WA PAKA.

❖❖❖❖

Naam..baada ya kuangalia kuhusiana na Mkojo wa Ngamia basi na tuangale na mfano mwengine wa ambao ni kuhusiana na Mkojo wa Mnyama mwengine ambae wengi sana hua tunamfuga Majumbani mwetu na Mnyama huyu si Mnyama mwengine yeyote isipokua ni Paka.

Ambapo aliulizwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana nao, na hivyo akajibu: **'Paka hua ni Tohara, kwani wao ni wale wanaotembea karibu yenu**.*' (Musnad Imam Ahmad, Sunnan Abu Daud, Sunan At Tirmidhii)*

Ambapo mbali ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Paka ni Mnyama Tohara kama ilivyosema Hadith lakini hata hivyo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wanasema kua:

Kama Paka atakaa kwenye sehemu, atalala kwenye Nguo n.k.

Bila ya Kuzikojolea wala Kuzinyea basi Sehemu hio na nguo hizo zitakua Tohara.

Lakini kama ikiwa atazikojolea Nguo au sehemu husika au ataitia Najis yeyoye ile basi Nguo au Sehemu hio itabidi itoharishwe.

Ambapo amesema Imam Ibn Aabidin Al Shaami kua: Mkojo, Kinyesi cha Paka na Panya hua ni Najis kulingana na Mtizamo uliokua Sahih,na hivyo huifanya sehemu na Maji yaliyoingia Ndani yake Najis hizo kunajisika.'*(Hashiyah Ibn Aabidin)*

Imam Ibn Abidin akasema tena kua: 'Kama ikiwa Paka atakunywa Maji au atakula chakula, basi hua ni Makruh kaa Ibn Adam kunywa au Kula kitu hicho alichobakisha na hii ni kulingana na Mtizamo ulio sahih, lakini pale itakapokua kuna njia nyengine lakini kama ikiwa hakuna njia

nyengine kutokana na kua Mhusika ni Masikini sana basi itaruhusika kula.'*(Hashiyah Ibn Aabidin)*

Na tunapoangalia kwa upande wa Madhhab ya Imam Muhammad Idris Al Shafii basi anasema Al Khatib Al Shirbini kua: **'Mkojo wa Paka ni Najis, hivyo kama Paka atakojoa kwenye sehemu basi itabidi sehemu itoharishwe kwa kumwagia Maji, hadi athari ya Najis iondoke.'**(Al Mughni Al Muhtaj)

Kwa maana hio basi kama akikokojole Nguo,Kiti, Zulia n.k basi itabidi Vitu hivyo vitoharishwe kwa kufuliwa.

Hapa sasa Mtihani unakuja kwenye Maduka na Maghala ya Vyakula ambamo mnakua na Panya wanaosambaa ovyo ambapo hukmu yake kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi hua ni kama kwa upande wa Imam Abu Hanifa.

Na kwa upande mwengine basi tumeona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoulizwa kuhusiana na Paka basi alisema kua ni Tohara na akatoa Sifa za Paka kua ni wenye kufuatana na Watu.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema hivi kwa sababu yeye Mwenyewe hakuwahi kufuga wala kua na Paka, kwani hakuna Hadith hata moja isemayo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua na Paka.

'Bali kuna hadith ya Ummu Ul Muuminin Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua Kulikua na Paka ambae alikua anakuja Nyumbani kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alikua akimiminia Maji kwenye Chombo na Paka huyo akaaa anakunywa na baada ya hapo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akatumia Maji hayo kutilia Udhu.'*(Hayat Al Haywan -Imam Ad Damiri)*

Naam..hivyo kama Mtu unafuga Paka na kisha Ukasikia Harufu ya Kijyesi au Mkojo wa Paka Nyumbani kwako, Kwenye Zulia, Kwenye Nguo, Chumbani, Kitandani, Kwenye viti, kwenye Sakafu, n.k

Basi itakubidi kutoharisha Nguo au sehemu husika kwa sababu sehemu hio haiko Tohara na hivyo haifai kukaa wala Kufanyia Ibada yeyote Juu yake kabla ya kutoharishwa kwake, mbali ya kua Paka ni Mnyama Tohara kulingana Na Makubaliano ya Wanazuoni Madhhab yote.

UMMUM UL BALWA NA MUBTILAT SALAT

❖❖❖❖

Na baada ya kuangalia kuhusiana na Ngamia na Paka basi na tuangalie kuhusiana na Kinyesi cha Ndege na Ummum Al Balwa au Mjumuisho wa Ugumu wa Kutoweza kueipuka Najis, kwani kama tulivyoona kua kulingana na Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni kua Wanafiqh wake wamesimamia kwenye Msimamo uleule wa kua Mkojo na Kinyesi cha Kila Mnyama na kila Ndege hua ni Najis. Na hii ni kutokana na Hadith tuliyoiangalia hapo kabla isemayo kua:

حَدَّثَنَا أَبُو نُعَيْمٍ، قَالَ حَدَّثَنَا زُهَيْرٌ، عَنْ أَبِي إِسْحَاقَ، قَالَ لَيْسَ أَبُو عُبَيْدَةَ ذَكَرَهُ وَلَكِنْ عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ الأَسْوَدِ عَنْ أَبِيهِ، أَنَّهُ سَمِعَ عَبْدَ اللَّهِ، يَقُولُ أَتَى النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم الْغَائِطَ، فَأَمَرَنِي أَنْ آتِيَهُ بِثَلاَثَةِ

أَحْجَارٍ، فَوَجَدْتُ حَجَرَيْنِ، وَالْتَمَسْتُ الثَّالِثَ فَلَمْ أَجِدْهُ، فَأَخَذْتُ رَوْثَةً، فَأَتَيْتُهُ بِهَا، فَأَخَذَ الْحَجَرَيْنِ وَأَلْقَى الرَّوْثَةَ وَقَالَ " هَذَا رِكْسٌ ".

Amesema Abu Nuaym kua ameseam Zuhayr kua amesema Abi Is-haq kua amesema si Abu Ubaydat aliesema bali ni Abdu Rahman Ibn Al Aswad kua amesema Baba yake kua amesema Jabir Ibn Abd *Allah Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alienda kujisaidia na kisha akaniomba mimi nimpelekee vijiwe vitatu.**

Nikatafuta Na kupata Vijiwe viwili nikatafuta cha tatu nikakosa hivyo nikachukua Kinyesi cha Mnyama Kilichokauka badala yake na kumpa. ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akachukua Vijiwe viwili na kisha akakirembea Kinyesi kikavu huku akisema: 'Hiki ni Kitu Kichafu.''** *(Sahih Bukhari, Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kwa Kawaida katika Madhhab yetu sisi ya Al Shafii basi kila Kinyesi na Mkojo Ni Najis Iwe kimotokana na Mnyama ambae ni Halali Kuliwa au Haramu kuliwa, na hii pia hua kwa Kinyesi cha Ndege wa Aina zote, Kinyesi cha Samaki, na Nzige, hata kwa Wanyama wasiokua na mfumo wa mzunguko wa Damu, hua ni Najis Kinyesi chao na Mkojo wao, na hii ni kulingana na Mtizamo Unaotegemewa kwa Usahihi Zaidi.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Ambapo hata hivyo runapozungumzia wale Wanaofuga Samaki kwenye Mabwawa kwa Mfano ambao Kinyesi cha samaki hao hua ndani yake Au Miskiti iliyo sehemu zenye Ndege wengi, na hivyo Kinyesi chao kiko kila sehemu, au Mjusi Au Nzige au Nzi n.k basi Hukmu yake hua inajumuishwa katika hali ya *Ummum Al Balwa.*

Ambapo anasema Imam Murtaza Al Zabidi kua: **'Kama inavyojulikana sana kua Ummum Al Balwa hua ni Mjumuisho wa maneno mawili ambayo ni Ummum linalotokana na neno A'am ambalo humaanisha Mjumuiko au Mkusayiko wa Pamoja, ambapo neno Balwa lnatokana na neno Bala lenya kumaanisha Ikhitbar yaani Jaribio au Mtihani'***(Tajj Al Arus)*

Na Imam Wahba Al Zuhayly Al Shami Al Shafii akasema kua**: 'Maana ya Ummum Al Balwa kulingana na Mtizamo wa Kishariah hua linamaanisha Jambo ambalo limeenea kwa wingi kiasi ya kua hua ni Vigumu kwa Mtu kujiepusha kutokana nalo, au kuachana nalo.**'*(Nadhariyyah Al Dharurah Al Shariyyah)*

Na kasema Imam Muslim al Dusari kua**: 'Ummum Al Balwa hua ni Kitu ambacho kinamjumuishia uzito kwa Mfanyaji Ibada, au hali ua Mfanyaji Ibada kua ni mwenye kufungika kutokana na uzito wa Jukumu juu ya kitu Fulani ambacho ni vigumu kukiepuka na hivyo kutowezekana kutekelezeka isipokua kwa kuongezeka kwa ugumu ambao unatakiwa usiwepo.'***(Darsah Nadhariyah)*

Na imesemawa katika Dhawabit Al Ikhityyar kua: **'Ummum Al Balwa humaanisha Tatizo kubwa sana ambalo linawatokea wengi miongoni mwa Wafanyaji Ibada au baadhi ya kikundi cha Wafanyaji Ibada katika Kupata urahisi wa Jambo ambalo hua linajirudia mara kwa mara na hivyo kua na ugumu zaidi kwao kuepukana nacho kitu hicho. Kwani kama wakiachana nacho basi watafikwa na Uzito zaidi'** (*Dhawabit al-Ikhtiar al-Fiqhiy in al-Nawazil*)

Hivyo kulingana na ufafanuzi huu basi tunaona kua Ummum Al Balwa hua ni kitu ambacho kinawasababishia Watu Ugumu zaidi wa mambo yahusuo Ibada kama wakitaka kuachana nacho au kuepukana nacho kitu hicho. Na kwa kua Malengo ya Sharia za Dinia kiislam hua ni kurahisisha Maisha ya kila Muumini katika Dini ya kiiislam kama zinavyosema aya:

﴿لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا﴾

La yukallifu Allahu nafsan illa wusAAaha*(Surat Al baqara 2:286)*

Tafsir: ***Haikalifishi Allah Subhanah wa Ta'ala Nafsi isipokua kwa Uwezo wake.***

Na kama alivyosema*Allah Subhanah wa Ta'ala :*

﴿مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ حَرَجٍ ﴾

Ma yureedu Allahu liyajAAala AAalaykum min harajin(Al Ma'idah: 5:6)

Tafsir: ***Hakutakieni Allah Subhanah wa Ta'ala kukujaalieni Ugumu***"

Na pia katika aya nyengine kua:

﴿وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ﴾

Wama jaAAala AAalaykum fee alddeeni min harajin*(Al Hajj: 22:78)*

Tafsir: ***Na Hajakujaalieni Allah Subhanah wa Ta'ala katika Dini yaliyo Magumu.***

Na pia zikasema aya kua:

﴿يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ﴾

Yureedu Allahu bikumu alyusra wala yureedu bikumu alAAusra*(Surat Al Baqara 2:185)*

Tafsir: ***Anataka Allah iwe rahisi kwenu na wala hataki iwe ugumu kwenu.***

Na akasema pia:

﴿ يُرِيدُ ٱللَّهُ أَن يُخَفِّفَ عَنْكُمْ وَخُلِقَ ٱلإِنسَانُ ضَعِيفاً ﴾

Yureedu Allahu an yukhaffifa AAankum wakhuliqa Al insanu dhaAAeefan*(Surat An Nisaa 4:28)*

*Tafsir:****Anataka Allah kukurahisishieni juu yenu, kwani amemuumba Mtu kua Dhaif.***

Hivyo Wanazuoni wameweka wazi hali ambazo zitambainishia Mtu kua jambo husika kama linajumuishika katika hali ya Ummum Al Balwa ama la, kwa kusema kua: '**Jambo husika ni lazima**

liwe linajumuisha idadi kubwa ya Watu kiuzito, hivyo hali hii hua si kwa ajili ya Mtu mmoja tu peke yake au kwa baadhi ya watu kidogo tofauti tu, kwa sababu Sharia za Kiislam hua ni zenye kuhusiana na hali ya Mjumuisho wa wengi.'

Kama alivyosema Imam Al Mawardi kua:

الْيَسِيرَ يَكُونُ تَبَعًا لِلْكَثِيرِ وَلَا يَكُونُ الْكَثِيرُ تَبَعًا لِلْيَسِيرِ

'Kilichokua Kidogo Kiidadi hua ni chenye kukifuata kilichokua Kingi kiidadi na haiwi kingi kua ndio chenye Kukifuata Kidogo.'*(Al Hawi A Kabir)*

Na kasema Imam Al Sarakhasi Al Hanafi kua:

الْأَكْثَرَ يُنَزَّلُ مَنْزِلَةَ الْكَمَالِ وَالْأَقَلُّ تَبَعٌ لِلْأَكْثَرِ

'Wingi huwekwa kwenye makazi ya Ukamilifu na Kidogo hua kinajumuishwa na kilichokua kingi'*(Al Mabsut)*

Hivyo kitu kinapokua kina maumbile ya mjumuisho wa kuwazidishia uzito wa kuwatokea Watu wengi basi hua na athari ya maamuzi ya kisharia na hivyo hua ni chenye kupelekea kitu husika kujumuishwa kwenye humu ya *Ummu Al Balwa* kulingana na Shariah, kama ilivyosemwa kwenye *Dhawabit Al Ikhtiyar Al Fiqhiy Al Nawazil* kua:

'Kwa Jambo husika lazima liwe ni lenye kuhitajika kufanywa kwa kurudiwarudiwa mara nyingi. Kwani kila Ibn Adam hua si mwenye kuhusi uzito kwa kitu ambacho hua anakitakiwa kukifanya mara moja tu au mara kadhaa lakini kwa kila baada ya kupita mda mrefu. Na hivyo kama ikitokea kutakiwa kukifaya kitu hicho mara kwa mara katka mda mfupi basi hua ni usumbufu mkubwa na uzito kwake, kwa hivyo kitu kinapokua kinajirudia mara kwa mara hua kinaingizwa kwenye mjumuisho wa Ummum al Balwa'.(*Dhawabit Al Ikhtiyar Al Fiqhiy Al Nawazil***)**

Ambapo tunapochukulia mfano wa Kuruhusika kupangusa Soksi za Ngozi (Al Khuf) katika wakati wa kutia Udhu wakati Mtu akiwa hayupo Safarini, ambapo kutokana na uzito wa kuzivua kila wakati wa kutia Udhu, aambapo hua ni Wajibu kuzivua katika wakati wa kukoga tu kama alivyosema Mujaddid Ad Din Imam Jalal Ad Din Al Suyuti Al Shafii katika Al-Ashbah wa Al-Nazair.

Na pia kama alivyosema tena Mujaddid Ad Din Imam Jalal Ad Din Al Suyuti Al Shafii kuhusiana na Wajibu **kitu ambacho hua hakiwezi kutofautishwa na udongo au uchafu ndani ya maji. Hivyo vyote hivi hua ni vigumu kuviepuka kwenye Maji na kutokana na ugumu huo basi Maji husika hua ni yenye kukubalika kutumika kwa ajili ya kujitoharisha hata kama yatakua yamebadilika kutokana na vitu hivi. Na hii ni kwa sababu kama Maji haya yatahesabiwi kua si Maji safi, basi hii itasababisha uzito kkwa sababu ni jambo la awaida kwa maji yanayokaa sana kua ni yenye kua na ukungu**.(*Al-Ashbah wa Al-Nazair to Al-Suyuti*)

Hivyo *Ummum Al Balwa* kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua ni Kitu ambacho chenye changamoto ya kutoepukika Kidini. Na hivyo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua**: 'Kitu kisichoepukika mbali ya kua ni Najis lakini huchukuliwa kua ni *Ummum Ul Balwa* yaani kinasitishiwa Hukmu yake kwa sababu ya Kutoepukia.'***(Al Majmuu)***

Na akasema Imam Sulayman Al Bujaraimi Al Shafii kua: **'Ummum Ul Balwa hii hua ni pale inapokua kuna Najis nyingi sana zaidi ya kawaida katika sehemu husika, kiasi ya kua kama Mtu atatafuta sehemu isiokua na Najis hio basi hua ni vigumu kwake kuipata na humuingizia kwenye Mashaka makubwa.'** *(Hashiyah Al Bujaraimi)*

Na akasema Imam Abu Bakr Shato Al Shafii kua: '**Ingawa Ni Sharti kua eneo la Kusali lazima liwe Tohara, lakini hata hivyo hua kuna kutoangaliwa sharti hili pale Inapokua katika sehemu husika Kuna Kinyesi Kisichoepukika cha Ndege, hivyo Najis hii hua inahesabika kua ni Ma'fu Anhu, pale itakapokua imeiathiri ardhi husika, au sakafu au Zulia, au Nguo, lakini katika hali zenye Masharti matatu yafuatayo**:

1-Pale Itakapokua Mtu husika hakukaa au hakupita katika sehemu husika kwa Makusudi.

2-Najis Hio isiwe katika hali ya Umaji maji, iwe Imekauka.

3-Najis hio iwe Haiepukiki.*(Hashiyah Inaya Talibin)*

Ambapo kwa upande wa Imam Abd Allah Al Ghaffar Al Qazwini Al Shafii basi amefafanua zaidi kwa kusema kua: **'Hata hivyo Kama Najis itakua mbichi ya Majimaji kama Kinyesi cha Ndege basi nayo pia huweza kutotiliwa Maanani pale itakapokua haiepukiki kabisa na hivyo Kumsababishia Mtu Mashakil.'**(*Al Ghurur Al Baghiyah Sharh Bahjah Al Wardiyah)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- KINYESI CHA NDEGE.

❖❖❖❖

Imesemwa katika Mawsuah Al Fiqhyyah Kuwaytiyyah kua**: 'Kinyesi wanachoangusha Ndege ambao Nyama yao inaruhusika kuliwa kama Njiwa na Vijumba Mshale huaa ni Tohara kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Madhhab ya Imam Malik na kulingana na mtizamo wa Madhhab ya Imam Hanbal, na hii ni kutokana na wngiwa kutapakaa kwake mabarabarani majumbani n.k na kutokana na Makubalianya Wanazuonikua Njiwa waachiwe Miskitini.**'

Ama kuhusiana na Kinyesi cha Ndege wasioruhusika Kuliwa kama Kipanga, Mwewe, Tai, Kunguru na mithili yake basi Wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Madhab ya Imam Malik, Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal ni wenye kukubaliana kua Ni Najis na hii ni kutokana na maumbile ya Ndege hao ambayo hupelekea Kinyesi chao kua ni chenye kunuka vibaya sana na Kuoza.

Ambapo kulingana na Mtizamo wa Imam Al Kharki basi ni kua ni Tohara kulingana na mtizamo wa Imam Abu Hanifa na Imam Abu Yusuf ambao ni mtizamo tofauti na Mtizamo wa Muhammad Ash Shaybani, ambapo wao wanatoa hoja ya kua Kinyesi cha Ndege hua hakina harufu Mbaya sana na hakuna Ndege ambae anatakiwa awekwe mbali na Msitiki, hivyo Kinyesi cha Ndege wote ni Tohara.

Ama kuhusiana na Mtizamo wa kua ni Najis kama wanavyosema wengi Miongoni mwa Wanazuoni, basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanasema kua: 'Wingi wowote ule wa Kinyesi cha ndege kama ukiingia kwenye Nguo au Mwili basi hua unasameheka kutokana na ugumu wa kujiepusha nayo au majaribio ya kujiepusha nayo, kwa mfano kama kwa ukubwa wa eneo la Dirham moja au chini yake.

Na Al Shafii amesema kua: Kinyesi kinapokua si kikubwa hua inasamehekana kudhaurilika kulingana na ugumu wa kuepukana nacho, na kama ni kngi basi hakisameheki kutokana na uadimu wake na pia ugumu wake wa kukiepuka.

Nao wanajua kuhusiana na Uadimu wake na wingi wake kutokana na maumbile ya Tabia na mazingira yake, kutokana na kile kinachoachwa na madoa yake na uguu wa kujiepusha nacho hua kidogo sana na zaidi yake.

Wanazuoni wa Madhhab Ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wanasema Kidogo ya kinyesi cha ndege hua haisameheki, isipokua pale itakapokua ni Damu kidogo au usaha kidogo tu ambao utakua si kinyaa kwa mtu. Ambaapo kuna nukuu kutoka kwa Ahmad isemayo kua hata idadi kidogo ya Matapishi, madhhii, Mate ya Punda, na Mate ya Wanyama wa Mwituni na Ndege.

Na Imam Abu Yaala amesema kua: 'Hukumu hii pia ni kwa ajili ya kInyesi cha Ndege kuokana na ugumu wa kijiepusha nacho''*(Mawsuah Al Fiqhyyah Kuwaytiyyah)*

Na akasema Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qalyubi Al Masri Al Shafii kua: '**Ndani yake mnaingia Pia kinyesi cha Ndege na Mkojo, vitu ambavyo hua ni Ma'fu anhu (Najis inayosameheka na kudharuliwa) hata kama ikitokea Nje ya Sala pale itakapoziathiri Nguo au Mwili, iwe Najis hio ni Kidogo au Nyingi, iwe Kavu au Mbichi iwe Usiku au Mchana kutokana na kua ni vigumu kuiepuka.'***(Hashiyah Al Qalyubi)*

Kwa maana hio basi kwa mfano kama inakua Najis ya Kinyesi cha Ndege, Mjusi, Nzige n.k, na kisha Mtu akaikanyaga Katika Kupita bila kukusudia au kutoepukika, au ikamdondokea kwenye Nguo, au kwenye Mwili basi hua Ni Najis ambayo inabidi iondolewe lakini hua hamna tatizo kwa sababu hua ni *Ma'fu Anhu* kutokana na kua *Ummum Al Balwa*, na hivyo hua haibatilishi Udhu wala Sala.

Au labda Mtu umechelewa Sala na kujikuta Umeunga Safu nje Msikitini na kisha Mbele yake ukakuta baka jeupe linalomaanisha Kinyesi kilichokauka cha Ndege, basi hua unaruhusika Kumalizia Sala yako.

Na tunapoangalia Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi tunaona kua wao wameigawa Najis itokanayo na Ndege katika Makundi yafuatayo:

1-Kwa Ndege aina ya Popo basi Mkojo wake na Kinyesi chake hua ni Tohara.*(Radd Al Mukhtar, Durr Al Mukhtar)*

2-Kinyesi na Mkojo wa Ndege wanaoruka Juu kama Njiwa, Kijumba Mshare, Kanga na Bata wa Majini hua ni Tohara. *(Radd Al Mukhtar, Radd Al Mukhtar)*

3-Kinyesi na Mkojo wa Ndege asieliwa iwe ndege huyo ni Muwindaji ama la, kama Kunguru, Kipanga, Mwewe, Tai,n.k hua ni Najis Khafifu.

Ambapo Hukmu ya Najis Khafifu basi ni kua kama ikiwa itaingia kwenye Nguo au mwili kwa wingi usiozidi robo ya Kiungo husika au Nguo husika basi Najis husika hua haina tatizo Na hivyo Udhu wa Mtu husika hautobatilika na wala Sala haitobatilika. **Lakini kama ikiwa ni sawa na Ukubwa wa Robo wa Kiungo husika cha mwili basi Udhu utabatilika.**

4-Kinyesi cha Ndege wasioruka kama Kuku na Bata wa Ardhini hua ni Najis Ghalizah yaani Najis Nzito, hivyo kama ikiingia kwenye Mwili au kwenye nguo kwa ukubwa wa Kuzidi Dirham Moja basi Udhu hubatilika na Sala hubatilika.

Na mtu atakaesali akiwa katika hali ya kua na Najis iliyochukua Ukubwa wa eneo la zaidi ya Dirham Moja basi mbali ya jua Sala yake ni Batili lakini pia hua ni Mwenye kufanya kufuru.

Na kama ikiwa Najis Ghaliza ina ukubwa wa Mzunguko wa Dirham moja kwenye Nguo au Mwili basi hua ni Wajibu kuitoharisha Nguo na Mwili husika, na kama Mtu akisali katika hali hio basi Itambidi airudie Sala hio baada ya Tohara ya Nguo na Mwili.

Na kuendelea na Sala katika hali hio bila Kujitojarisha hua ni Kufanya Dhambi Na Najis Ghaliza ikiwa imechukua eneo dogo zaid ya Dirham basi hua ni Sunnah kuisafisha sehemu husika, na kama Mtu akisali nila kuisafisha basi ingawa Sala yake hua Sahih, lakini hua ni bora kuirudia.'(*Bahr Shariat)*

Na akasema Al Allamah Al Muhaqqiq Imam Ibn Aabidin Ash Shami kua: **'Ama kwa Ndege wasioruka kama Kuku na Bata basi Kinyesi chao na Mkojo wao hua ni Najis kubwa na hivyo humaanisha kua kama Ukisali huku ukiwa uzito wa Gram 5 za Najis hio Kwenye Nguo au mwili au sehemu unayosalia basi Sala hua batili.**

Na hukumu hua hio hio pale Najis hio itakapofikia mzunguko wa sentimita 5 katika kutawanyika kwake na hivyo itabidi Utoharishe sehemu husika. **Na kusali na Najis isiyozidi sentimita 5 au gramu 5 basi hua inakirihisha lakini sala yako itakua Sahih.**

Ama kuhusiana na Ndege wanaoruka basi kuna waliokua halali kuliwa ambao Kinyesi chao na Mkojo wao hua Tohara iwe kwenye nhuo au mwili wako.

Na kuhusiana na Ndege wanaoruka lakini ni haram kuliwa basi Udhu hautobatilika pale itakapokua Najis husika haikufikia ukubwa wa Robo wa sehemu husika au kiungo husika cha mwili. **Ama kuhusiana na Kinyeshi chao kama kikiingia Kisimani tuseme basi Maji ya Kisima yatakua Tohara kutokana na Ugumu wa Kukitoharisha na kukilinda Kisima kisingie Najis hio.'***(Radd Al Mukhtar)*

Ambapo hapa katika Hukmu ya Kisima tunaona kua imetumika pia Kanuni ya *Ummum Al Balwa.*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi anasema Imam Ahmad Ad Dardir Al Maliki kua: '**Na miongoni mwa vitu ambavyo ni Tohara hua ni Kinyesi cha Ndege lakini pale itakapokua Ndege huyo hakula kitu ambacho ni Najis.'***(Sharh Al Saghir Ala Aqrab Masalik Ila Madhab Maliki)*

Kwa maana hio basi kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik tunaona kua Kinyesi cha Ndege wanaoruhusiwa Kuliwa hua ni Tohara isipokua kama Ndege husika atakua amekula Najis. Au amelishwa Najis, na hivyo kutokana na kua Chakula alichokula ni Najis basi ni Kinyesi chake pia hua ni Najis.

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa ambae ni Imam Muhamad Ibn Hasan Ash Shaybani Al Hanafi.

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi Mtizamo wao ni kua Kinyesi cha Wanyama wote wanaoruhusika Kuliwa hua ni Tohara wakiwemo ndege pia.

Lakini kwa Wanyama wasioruhusika kuliwa basi Kinyesi na Mkojo wao hua ni Najis.

Kama anavyosema Imam Mustafa Ibn Saad Abd A Suyuti Al Ruhaybaani Al Dimashq Al Hanbali kua: '**Ama kuhusiana na Mkojo na Kinyesi cha Ndege wasioruhusika kuliwa kama Popo n.k hua ni Najis.'**(*Matalib Uli Nuuha Fi Sharh Ghayat Al Muntaha)*

Kwa maana hio basi kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal tunaona kua: '**Kama ikitokea kua Mtu amenyewa au amekojolewa na Ndege walio halali kuliwa, au labda sehemu anayosalia imekutwa na Kinyesi cha ndege anaeliwa, basi hua hakuna Ulazima wa Kusafisha Nguo husika, au sehemu husika ya kusalia, kwani hakuna tatizo kusalia nguo hio au kusalia sehemu hio.'**

Kama anavyosema Muwafaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali Kua: **'Mkojo na Kinyesi cha Wanyama wanaoliwa hua ni Tohara, ambapo huu ni Mtizamo wa Imam AlKharqi, Imam Ata'a, Imam An Nakhai, Imam Sufyan Ath Thawry na Imam Malik, na Imam Malik amesema kua: 'Wanazuoni hawauhesabu Mkojo wa Mnyama ambae ni Halali kuliwa na Maziwa yake kunywewa kua ni Najis, na Imam Al Zuhri na Imam Yahya Al Ansari wameruhusu Mkojo wa Kondoo. Na Imam Abu Jafar, Imam Al Hakam na Imam Hammad na Abu Hanifa wameruhusu Kinyesi cha Ndege kua ni Tohara'***(Al Mughni)*

Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali anaendelea kutuambia kua : '**Ama kuhusiana na Kinyesi na Mkojo wa Ndege ambae Nyama yake hailiwi kwa mfano kama Ndege wenye kuwinda kwa Kucha kama Kipanga n.k basi Kinyesi chao na Mkojo wao hua ni Najis na hakuna Kupingana kwa Wanazuoni juu yake Jambo hilo.'**

Kwani Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Al Shafii na Imam Abu Thawry na Imam Al Hasan wamesema kua Kinyesi chaa Ndege hua ni Najis kwa sababu kimejumuishwa kwenye maana ya maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pale aliposema kua: Jiepusheni na Mkojo kwani takriban ya adhabu yote ya kaburi hua ni kutokana na mkojo. Na kwa sababu Mkojo ni Najis na hua ni sawa na Kinyesi cha Ibn Adam.'*(Al Mughni)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- MANYOYA YA NDEGE

❖❖❖❖

Naam..wengi Miongoni mwa watu ni wenye kupenda kufuga Ndege wakiwemo Njiwa, Kasuku, Bata, Kuku n.k

Na inawezekana kua wengi ni wenye kujua na pia si wenye kujua kuhusiana na Utohara au Unajis wa Manyoya Ndege wanaowafuga mbali ya kua hili ni moja kati ya Mambo Muhimu kwa kila Muislam pale unapowadia mda wa kuwasiliana na Mola Wake, yaani katika wakati wa Ibada ya Sala.

Na ingawa tumeona kuhusiana na Kinyesi cha Ndege na hukmu ya *Ummum Ul Balwa* , ambapo hata hivyo wengi hua ni wenye kujua kuhusiana na Kinyesi kua ni Najis, hivyo na tuangalie kuhusiana na Manyoya ya Ndege ambayo kwa upande wake hua hayana Hukumu ya kujumuishwa kwenye *Ummum Al Balwa* kutokana na kua Mtu unaweza kuepukana nayo na kujitenga nayo bila ugumu wa tatizo lolote.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua wao wanasema kuhusiana na Manyoya kua hukumu yake ni kua: **'Hua inategemeana na aina ya Ndege kwani kama ndege husika ni Halali kuliwa basi na Manyoya yake yatakua Tohara, lakini kama ni Haramu basi Manyoya yake hua ni Najis.'**

Ambapo Najis ya Manyoya ya Ndege husika ambae nu Haram kuliwa hua ni Najis pale yatakapokua yameroa na kisha yakagusa Nguo zako, au ngozi yako au sehemu unayosalia. **Ambapo Unajis wa Manyoya tunaouzungumzia hua ni pale yanapotoka kwenye mwili wa Ndege husika na kua peke yake, na yakawa yameroa basi huwabinisha kutoharishwa kwa sehemu husika, au Nguo Husika au Kiungo husika cha Mwili kilichogusa.**

Lakini kama Manyoya hayo ni Makavu na hayakuroa basi ingawa pia hua ni Najis lakini hua hayawajibishi kutoharisha kitu kilochoguswa nayo, yaani kama limekaa kwenye Msala, Nguo au Mkononi mwako basi utaliondoa na kusali

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: **'Kama Manyoya, Nywele au Sufi itakua zimetengana na Mnyama ambae ni Halali kuliwa, iwe kutengana nae huko hua ni kutokana na kuchomolewa, Kunyonyolewa au Kunyonyoka yenyewe, basi kuna Mitizamo miwili tofauti juu yake. Ambapo Mtizamo uliokua sahih zaidi ambao ni Mtizamo wa Imam Al Haramayn, Imam Al Baghawi na wengi Miongoni mwa Wanazuoni basi ni kua ni Tohara''***(Al Majmuu)*

Na kisha akasema tena Imam An Nawawi kua: **'Kama ikiwa Nywele, Manyoya au Sufi za Mnyama ambae ni Haram kuliwa yakikatwa, Yakinyonyolewa au yakitoka yenyewe, basi Wanazuoni wetu wanakubaliana juu yake kua yanajumuishwa sawia na Nywele au Manyoya ya Mnyama aliekufa.**

Kwa sababu chochote kile kilichokatwa kutoka kwa Mnyama aliekua Hai basi hua Nyamafu. **Na hivyo kinachofuatia hua makubaliano ya kutokukubaliana tulikokutaja hapo kabla kuhusiana na Manyoya au Nywele za Mnyama aliekufa kupitishwa Hukmu yake ambayo ni kua Kila Kitu kilichotengana na Mnyama wake hua ni Najis, isipokua pale Mnyama huyo atakapokua ni Ibn Adam ambacho hua ni Tohara.'***(Al Majmuu)*

Naam..nadhani tufafanue hapa kidogo kwa Mfano wa Ndege aina ya Kasuku. Hivyo Kama ikiwa kuna Kasuku amekatika Mdomo wake au kucha basi kwa kua Kasuku haliwi basi na Mdomo wake au kucha yake itakua ni Najis. Na kama Kasuku akitoka Manyoya kutokana na Kujikuna au Kunyonyolewa au Kukatwa basi Manyoya hayo yatakua ni Najis na itabidi yafagiwe kabla kusalia sehemu husika.

Na kama yakiingia Maji katika sehemu yalipoangukia basi sehemu husika hua si Tohara itabidi itoharishwe, na kama Kuna nguo Imefuliwa labda na kisha nyoya hilo likaangukia Nguo hio imaji nalo likaroa basi itabidi nguo ikafuliwe tena. Au Nyoya hilo limaji likakuangukia kwenye Nguo Uliyovaa basi Nguo haitofaa Kusalia kwani imeshaingia Najis n.k

Miongoni mwa masuali ambayo baadhi hua wanajiuliza ni kua Kuna baadhi ya Watu hua ni wenye Kuweka Nyoya la Tausi Ndani ya Msahafu ama Juzuu kutokana na uzuri wake na hivyo kutumia kama alama ya mtu kuiikumbusha kua amefikia Ukurasa gani. Hivyo Jee Manyoya ya Tausi ni Tohara ama Najis? Kwani kama ni Najis basi hua ni Haram kuliweka Ndani ya Qur'an.

Naam..jibu la suali hili tunalipata kwenye Hadith ya Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* isemayo kua:

عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ قَالَ نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَنْ كُلِّ ذِي نَابٍ مِنَ السِّبَاعِ وَكُلِّ ذِي مِخْلَبٍ مِنَ الطَّيْرِ.

Amesema Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **amekataza Kuliwa kwa kila Mnyama Muwindaji mwenye Meno Yenye Ncha Kali na Kila Ndege Mwenye Kucha Kali za Kuwindia'** *(Sahih Muslim, Mishkat Al Masabih)*

Na kwa maana hio basi Ndege aina ya Tausi hua hayumo kwenye Sifa hizi na hivyo Tausi Ni Halali kumla. Kwani imesemwa kwenye *Mawsuat Al Fiqhiyyah Kuwaytiyyah:* **'Mtizamo wa wengj Miongoni mwa Wanazuoni basi ni kua Manyoya ya Mnyama ambae ni halali kuliwa hua ni Tohara, hata kama ikiwa wamekufa.'(***Mawsuah Al Fiqhiyyah Al Kuwaytiyyah)*

Na kutokana na kua ni Halali Kumla basi Manyoya yake hua ni Najis bali hua ni Tohara na hivyo inaruhusika kuweka ndani ya Msahafu kama wawekavyo wale wapendao kufanya hivyo kutokana na Uzuri wa Manyoya hayo. Kisha ikasemwa tena kwenye *Al Mawsuah Al Fiqhiyyah Al Kuwaitiyyah* kua: **Ama kuhusiana na Ndege ambao ni Haram kuliwa basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na wa Madhhab ya Imam Malik hua ni wenye kuyachukulia Manyoya ya Ndege hao kua ni sawa na Ndege ambao ni Halali kuliwa yaani kua ni Tohara**.

Lakini kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao Mtizamo wao ni Kua Manyoya ya Ndege ambao ni Haram kuliwa hua ni Najis, kwani imesemwa kwenye Al Mughni kua: Nywele, Manyoya ya kila Mnyama hua ni sawia na Sehemu nyenginezo za Viungo vya Mwili wake. **Hivyo kila kilichokua Tohara basi Nywele zake na Manyoya yake hua ni Tohara**. **Na kila kisichokua Tohara basi na Nywele na Manyoya yake hua ni Najis na hakuna utofauti kama Mnyama huyo yuko hai au amekufa.'***(Al Mawsuat Fiqhiyyah Kuwaitiyyah)*

Na ikasemwa tena kua**: Wanazuoni Wanakubaliana kua Manyoya hua ni Sawia Kihukumu na Nywele na vinafanana, na Wanakubaliana kua Manyoya ya Ndege wanaoliwa hua ni Tohara pale yanapokua kwenye Ndege mwenyewe wakati akiwa hai**. **Na pia kama yakkanguka au yakinyonyolewa basi wengi Miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua ni Tohara na Uthibitisho wao na Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo kua;**

﴿وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُم مِّن بُيُوتِكُمْ سَكَنًا وَجَعَلَ لَكُم مِّن جُلُودِ الْأَنْعَامِ بُيُوتًا تَسْتَخِفُّونَهَا يَوْمَ ظَعْنِكُمْ وَيَوْمَ إِقَامَتِكُمْ ۙ وَمِنْ أَصْوَافِهَا وَأَوْبَارِهَا وَأَشْعَارِهَا أَثَاثًا وَمَتَاعًا إِلَىٰ حِينٍ﴾

WaAll<u>a</u>hu jaAAala lakum min buyootikum sakanan wajaAAala lakum min juloodi al-anAA<u>a</u>mi buyootan tastakhiffoonah<u>a</u> yawma *<u>dh</u>*aAAnikum wayawma iq<u>a</u>matikum wamin a<u>s</u>w<u>a</u>fih<u>a</u> waawb<u>a</u>rih<u>a</u> waashAA<u>a</u>rih<u>a</u> ath<u>a</u>than wamat<u>a</u>AAan il<u>a</u> <u>h</u>eenin(*Surat An Nahl 16:80)*

Tafsir: ***Na Allah Amejaalia kwa ajili yenu Katika Makazi yenu Utulivu Amekujaalieni juu yenu Kutokana n Ngozi za Wanyama (Mahema) Makaazi Ambayo Mnayahisi Malaini na yenye Kuvutia Katka Siku Mnapokua Safarini na katika Siku mnapopiga Kambi naKutokana na Sufi zao, Na Manyoya yao Na Nywele zao Kua ni Fanicha na Vitu vya Ndani vya Ndani ya Majumba vyenye kukuridhisheni kwa Mda mchache.***

Subhanah Allah wa bihamdihi La Ilaha Illa Allah wa Allahu Akbar!!
Naam..kusema kweli hii ni aya moja ambayo ufafanuzi wake tu basi ni mada inayojitegemea, na hivyo tunaachana nayo kiufafanuzi na kurudi nayo kama ilivyosemwa kwenye Mawsuah Fiqhiyyah kua**: 'Hukmu iliyomo ndani yake ambayo ni yenye uthibitisho wa kua Aya hii imetaja Nywele za Wanyama ambazo ni zenye kuenda sambamba na Manyoya ya Ndege, na hivyo kama ingekua**

Manufaa ya Wanyama ni kutokana na Nyama tu, basi Manyoya na Nywele na Sufi zingepotea bure.

Ambapo Baadhi ya Wanazuoni wamesema kua aya hii ni Moja kati ya sehemu mbili za Sunna zilizobainishwa na Qur'an. **Ambao ni Mjumuisho wa Hadith ya *Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam* pale aliposema: 'Kile kilichokatwa kutoka katika Mnyama aliekua Hai Basi hua ni Maiti" hivyo hii imebainishwa na maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo: Na kutokana na Sufi zao na Manyoya yao na Nywele zao**. **Hivyo Kulingana na Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni ni kua Manyoya ya Ndege anaeliwa hua ni Tohara***(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaitiyyah).*

Na kwa kua Wanazuoni wanakubaliana kua Manyoya ya Ndege Waliokua Halali Kuliwa kua ni Tohara, basi hukmu hii ya Manyoya pia ni hukmu inayoenda sambamba na Hukmu ya Nywele, Sufi na Ngozi za Wanyama wanaoliwa.

Kwani amesema Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii kua: '**Amesema Imam Al Shafii kua: Mtu anaruhusika Kusali Kwenye Ngozi ya Mnyama ambae ni Halali kuliwa pale atakapokua amechinjwa, na pia anaweza kusali kwenye Sufi, Nywele na Manyoya yake kama Ikiwa Yamechomolewa kutokana nae wakati akiwa Mzima.'***(Al Hawi Al Kabir)*

Imam Al Mawardi anaendelea kusema kua: '**Hasan Al Basr Alisema kua: Katika wakati wa kipindi cha Baridi basi Masahaba wa *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* walikua wakinukia kama harufu ya Kondoo kutokana na Nguo za Manyoya ya Kondoo walizokua wakivaa.**

Kwa sababu Manyoya hua yanachukuliwa kutokana na Mnyama anaeliwa Nyama yake kutokana na Manufaa yake, na yanaruhusika kama Maziwa, na tunaposema Manufaa hua tunamaanisha Kuchukuliwa bila Kukataa kiungo cha Mnyama husika.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Na kwa kua kwa upande wa Ndege wasioliwa basi Kuna Kutofautiana juu yake Kwani kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahu Hanifa na Imam Malik basi Wanasema kua ni Tohara,

Lakini kwa upande wa Wanazuoni Madhhab ya Imam al Shafii na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal Basi Wanasema kua Ni Najis.

Na hivyo tunaweza kujiuliza Jee kwa mtu asiejua kama Nyoya la Ndege husika ni Tohara ama ni Najis na limemuangukia Nyoya ambalo limeroa maji nae ametia Udhu. Jee Hukmu yake ikoje? Ambapo Suali la Jibu hili hua ni Kua kwa kua Mtu Hajui na ana shaka basi Kisharia Unyoya Huo hua ni Tohara

Na mbali ya kua Wanazuoni wanakubaliana kua Wanazuoni Wanakubaliana kua Unyoya wa Ndege ambae ni Halali kuliwa hua Tohara

Lakini Kama ikiwa ndege husika hakuchinjwa kwa Njia ya Kiislam au amekufa bila ya Kuchinjwa basi Manyoya yake hua ni Najis hata kama Ndege huyo ni halali kuliwa na hii ni kwa sababu Uharamu wake unatokana na Kuchinjwa bila kutajiwa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala*

Ila anasema Imam Al Muhaqqiqin Al Aalama Al Faqih Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: '**Kama ikiwa Mtu atakua na Shaka kuhusiana na Chanzo cha Manyoya Ya Ndege husika kama Yametoka baada au kabla ya Kuchinjwa, basi Kiasili Hukmu yake hua ni kua Manyoya hayo ni Tohara.'***(Tuhfah Al Muhtaj).* Ambapo huo pia ndio Mtizamo ulioelezewa na Al Khatib Al Shirbini katika Al Mughni Al Muhtaj

Na baada ya kuangalia kuhusiana na Hukmu Utohara na Unajis wa Kinyesi cha Ndege na Manyoya ya Ndege kulingana na Mitizamo ya Wanazuoni mbali mbali. Hivyo tumalizie kuhusiana navyo vitu hivi kwa kuangalia hali ziifuatazo:

Tuseme Mtu alikua anasali na Kisha baada ya Kusali akajikuta kua kumbe kwenye Nguo yake, kuna Kinyesi cha Ndege, ambae ni Najis kama Kunguru, au labda Mgongoni amejikuta amegandwa na Nyoya la Ndege asieliwa na hivyo kua ni Najis Jee Hukmu yake ikoje?

Ambapo kwanza tukumbushane kua Kama Ikiwa Ni Nyoya ambalo ni Kavu basi Sala iko Sahih. Lakini kama ikiwa Nyoya lina Maji na ni la Ndege asieliwa na wewe ulikua Unajua juu yake basi katika hali kama hii Sala yako Itakua Ni Batili, hivyo itakubidi uirudie Sala hio baada ya Kutoharisha Nguo yako au sehemu ya mwili liliugusa kutokana na Najis ya Nyoya hilo.

Ila kama ikiwa Mtu amesali hadi akamaliza bila kujua juu ya Najis hio basi hua kuna Mitizamo Mitatu juu yake ambayo ni:

1-Katika Hali kama hii basi Sala ya Mtu husika ha hijabatilika,ambapo huu ni Mtizamo wa Abd Allah Ibn Umar Radhi Allahu Anhu, Imam Ataa, Imam Said Ibn Al Musayyib, Imam Salim, Imam Mujahid, Imam Abd Rahman Al Shabi, Imam Al Zuhri, Imam Is-haq Ibn Rahawayh Al Shafii, Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii, na pia kuna kauli Moja ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

2-Katika Hali kama hii basi Mtu Husika atatakiwa Kuirudia Sala yake baada ya Kua Tohara, ambapo huu ndio Mtizamo Unaokubalika wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, na wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

3-Katika Hali kama hii Basi Mtu husika atatakiwa kuirudia Sala yake pale itakapokua Wakati wa Sala hio haujamalizika, na Kama Umeshapita basi haina haja ya kurudia, ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Malik na Imam Rabiah *(Al Majmuu, Al Mughni na Hashiyat Al Dasuqi)*

Ambapo anasema Imam Abu Al Husayn Yahya Al Amran Al Shafii kua**: 'Kama ikiwa Mtu alijua kuhusiana na Najis husika na alikusudia Kujitoharisha kabla ya Ibada ya Sala lakini akasahau, basi Sala yake itakua Batili kwa sababu ya Kutojali kwake.'***(Al Bayan Fi Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Imam Al Imran Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Kama ikiwa hakujua kuhusiana na Najis hio kama aliipata baada ya Sala au ndani ya Sala basi kwanza anatakiwa atafakkari. Kwani kama ikiwa ameipata baada ya Sala basi haitomlazimu kuirudia Sala, kwa sababu kiasili ni kua hakua na Najis hio katika wakati wa Sala, lakini inapendekezwa kuirudia Sala kwa sababu huenda ikawa ameipata wakayi akiwa ndani ya Sala Na Kama ikiwa inawezekana kua aliipata ndani ya Sala basi hua kuna Mitizamo miwili juu yake ambapo kwa kwanza ni kua:**

Haina haja kwake Kuirudia Sala, ambapo huu ni Mtizamo wa zamani wa Imam Al Shafii wenye kulingana na ile hadith isemayo kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alivua viatu vyake wakati akiwa ndani ya Sala. Hivyo Masahaba nao wakavua viatu vyao, na baada ya kusali *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawauliza: Kwanini mmevua? *Masahaba Radhi Allahu Anhum* wakasema: Kwa sababu Sisi tumekona wewe umevua viatu hivyo nasi tukavua.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Mimi nilivua kwa sababu Malaika Jibril alinijia akaniambia kua kwenye viatu vyangu kuna uchafu. Hivyo Hadith hii inatuonesha kua kam Sala ingekua Ni batili basi angeamarisha Kusaliwa tena Sala hio.**

Na Mtizamo wa pili ambao ndio Mtizamo mpya wa Imam Al Shafii na ndio Unaotegemewa zaidi basi ni kua Sala hio inabidi irudiwe tena upya kwa sababu Utohara wa Kimavazi hua ni Wajib na hauondolewi kutokana na Ujinga, kama Udhu.'*(Al Bayan Fi Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Na tuseme kua kuna Mtu amesahau Kitu kama Kitambaa cha Mafua, Tissue n.k ambacho Kina Najis ndani ya Mfuko wa Nguo yake na amekumbuka ndani ya Sala juu yake jee afanyeje?

Ama juu ya hili basi kwanza Sala husika Hubatilika, hivyo itambidi akitoe Kitu hicho chenye Najis na akiweke mbali nae. Hivyo anasema Imam Shamsu Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Ramli Al Shafii kua: '**Kama ikiwa kuna jambo la kutakiwa kuchagua baina ya Kuitupa Najis husika ili Sala yako iwe Sahih, lakini huna sehemu ya kuitupia kwani uko ndani Msikitini, na hivyo itakubidi Uitupie humo humo ndani Msikitini, au usiitupe Ndani Msikitini kwa sababu ya Kuogopa kuweka uchafu Msikitini,lakini itakubidi Ubatilishe Sala yako, basi Mimi nadhania kua ni Bora Kuilinda Sala Yako kwanza kwa kukitupa pembeni Kitu hicho ndani Msikitini ili ukishamaliza Kusali basi ukiokote ukakitupe nje, kwa sababu kufanya hivyo itakua Umehifadhi Sala yako na pia Umehifadhi Usafi wa Msikiti, kwa sababu hua inaruhusika kuitupa Najis pembeni na kuikawilisha uondowaji wake hadi utakapomaliza Kusali kutokana na Dharura.'***(Nihayat Al Muhtaj)*

Naam..tumemalizana kuhusiana na Kufisidika kwa udhu kutokana na Manyoya ya Ndege ambapo bila ya Shaka katika Kuzungumzia kwangu kwa upande wa Mitizamo ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi ingawa nimekua nikimnukuu sana Imam An Nawawi lakini pia nimekua nikihama hama kwa Imam Al Mawardi, Imam Al Rafii, Imam Al Ramli, Imam Zakariyah Al Ansari, Imam Ibn Hajar Al Haytami,Imam Al Bujaraimi, Imam Al Imran n.k. Hivyo kwa kua inawezekana kua ikawa naonekana kua nimeegemea sana kwa Imam An Nawawi zaid basi kuna jambo ambalo inabidi tulibainishe kidogo kabla ya kuendelea zaid.

Na jambo hilo ni kua: Kihistoria hapo awali Katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi kutokana na Maisha ya Imam Al Shafii, ambayo aliianza kuishi kuanzia Gaza nchini Palestina alipozaliwa Mnamo mwaka 150 Al Hijra, Na kisha akahamia Mjini Makkah pamoja na Mama yake alipokua na Umri wa miaka miwili baada ya kufariki Baba yake

Hivyo Msingi wa Elimu yake ya kwanza Imam Al Shafii aliipatia Mjini Makkah kabla hajahamia Madina kwa Imam Malik, ambapo baada ya Kufariki Imam Malik mnamo mwaka 180 Al Hijra basi Imam Al Shafii akarudi Mjini Makkah na kuanza Kua Imam anaejitegemea.

Baadae akahamia Yemen, kisha Baghdad kisha akarudi Makkah kisha Akarudi tena Makkah, kisha akarudi tena Baghdad, ambapo mote humo alikua katika njia ya kutafuta Ilm na kueneza Ilm, na kua na Wanafunzi kama Imam Ahmad ibn Hanbal na Imam Is-haq Ibn Rahwayh. N.k

Hivyo katika Kipindi hiki Imam Al Shafii alikua akitoa Fatwa, ambazo zinapatikana kwenye Kitabu cha Al Risala ambazo zinajulikana kama Mtizamo wa Zamani wa Imam Al Shafii, au Al Qawl Al Qadim

Kisha mnamo mwaka 196 Al Hijra Imam Al Shafii alihamia nchini Misri kwa ajili ya kusoma kwa Imam Al Layth Ibn Saad lakini alipowasili Misri Imam Al Layth akawa ameshafariki, hivyo Imam Al Shafii akabakia Nchini Misri hadi mwaka 204 Al Hijra alipofariki Dunia, na Kuacha Wanafunzi, kina Imam Al Muzani, Imam Al Buwayti, Imam Al Rabi n.k na Vitabu kadhaa vikiwa Al Umm

Ambapo Kitabu cha Al Umm ndio Kitabu cha Mitizamo Mipya ya Imam Al Shafii au Al Qawl Al Jadid

Hivyo ndio ikawa kuna Kauli ya zamani na kauli mpya. Na tofauti ya mitizamo baina yake ni katika mambo 18, ambayo hapa hatuyazungumzii kwa sababu ni mada nyengine, ila kwa anaetaka kujua zaidi atafute kitabu changu cha Ijithad na Taqlid kinapatikana bure mtandaoni.

Na baada ya kufariki Imam Al Shafii basi Wanafuni wake wakatawanyika hivyo ikawa kuna Mitizamo miwili tofauti ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kwani kuna Skuli ya Fiqh Misri na Kuna Skuli ya Fiqh ya Khurasan.

Ambapo hali hii iliendelea Hadi alipokuja Mujadidd Ad Din Imam Al Ghazali miaka 350 baada ya kufariki Imam Al Shafii ambae ndie alieziunganisha Fiqh hizi za pande mbili na kuzifanya kua katika sehemu moja kwa kutoa vitabu vya Al Basit, Al Wajis na Al Wasit.

Ambapo tulisema kua hivi ndio Vitabu Mama vilivyofafanuliwa na Mashaykh Wawili ambao ni Imam An Nawawi na Imam Al Rafii.

Kwa maana hio basi Katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kuna Wahakiki wakuu wawili ambao ni Imam An Nawawi na Imam Al Rafii.

Na kisha baada ya Maimamu wawili hawa basi kuna Wahakiki wawili wengine wa Fatwa za Maimamu wa Madhhab zote, ambapo wa kwanza ni Imam Ibn Hajar Al Haytami, na wa pili ni Imam Al Ramli.

Hivyo kulingana na Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua Kama ikiwa Imam An Nawawi na Imam Al Rafii wamekubaliana juu ya Jambo husika, basi Jambo hilo litakua ndio lenye kutegemewa.

Na kama wakitofautiana basi Mtizamo wa Imam An Nawawi hua unapewa kipaumbele zaidi kuliko Mtizamo wa Imam Al Rafii, mbali ya kua inawezekana kutumia mitizamo ya wote wawili katika jambo husika.

Na kisha wanafuatia wahakiki wawili ambao ni Imam Ibn Hajar Al Haytami na Imam Al Ramli, ambapo Kama ikiwa Imam An Nawawi na Imam Al Rafii hawakutoa Fatwa juu ya Jambo husika basi kama ikiwa watakubaliana Imam Ibn Hajar al Haytami na Imam Al Ramli juu ya Jambo hilo basi jambo hilo litapita na Kukubaliwa kua ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Na kama ikiwa Imam Ibn Hajar Al Haytami na Imam Al Ramli watatofautiana, basi hapa kutakua na kutofautiana kimtizamo baina ya Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii hata leo hii kwangu mimi na wewe kwa ujumla.

Na hii ni kwa sababu Wanazuoni wawili hawa wakitofautiana baina yao Kimtizamo basi Wanafiqh wa Madhhab Imam Al Shafii wa Hijaz na Yemen, Mashariki ya mbali na Afrika Mashariki hua wanafuata Mtizamo wa Imam Ibn Hajar Al Haytami.

Na Wanafiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii wa Misri na Sham yaani Palestina, Syria, Jordan, Lebanon, Uturuki na hadi nchi za Kialam za Kirusi pia hufuata mtizamo wa Imam Al Ramli.

Naam..hivyo ndivyo hali halisi ilivyo ambayo inayonipelekea kurukaruka kwa Maimamu na kuelema zaidi kwa Imam An Nawawi na Ibn Hajar Al Haytami pia.

MUBTILAT SALAT – MAA'DHUR UDHU WA WENYE UDHURU.

❖❖❖❖

Kwani kama tulivyoona hapo kabla tulipozungumzia kuhusiana na Damu ya Istihadha kua Kimaumbile kuna watu ambao hua na Matatizo ya kutoweza kudumu na Udhu, kutokana na kua na Matatizo ya Kiafya kama Ya Kutokwa na Damu kwa Wanawake au Kutoweza kuuzuia Mkojo kwa Wanaume na Wanawake kutokana na Ukubwa wa Kiumri, Kua na tatizo la Gesi ya Tumbo na hivyo kutozuilika kutoka kwa gesi tumboni, au Kutokwa Kinyesi, au Manii, Madhi, Madii n.k.

Na mbali ya kua baadhi ya wakati Matatizo haya huwapata Watu wazima Kiumri lakini baadhi ya wakati hadi vijana pia kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo Matatizo ya Kiafya. Na hivyo Watu wenye Matatizo haya hua wanajulikana kama Ma'adhur kutokana na kua ni Wenye Udhuru.

Ambapo Tatizo la Ma'adhur hua ni lenye kuanza kuingizwa kwenye Hukmu pale inapokua Mtu ana hali ya kutoweza Kukaa na Udhu kuanzia ndani ya Kipindi cha Sala moja hadi Nyengine, kutokana na Tatizo la Kushindwa Kujidhibiti na kujizuia na hivyo kua ni mwenye kutokwa na Damu, Mkojo, Kinyesi, Gesi, Usaha n.k katika Tupu ya Mbele au ya Nyuma. Na hivyo kutokana na Udhuru wa Mtu Husika basi hua anatakiwa kusimamia Mambo yafuatayo:

Anatakiwa Kujitoharisha Kutokana na tatizo la Najis aliyokua nayo katika Wakati huo, lakini Tunapozungumzia kuhusiana na tatizo linapokua ni Gesi basi hii haimaanishi kua anatakiwa ajisafishe katika Utupu wa Nyuma la! Kwa Sababu Kufanya Hivyo hua ni Makruh kama ilivyosemwa na Imam Sayyid Ahmad Ibn Umar Al Shatiri al Alawi Al Tarimi Al Shafii katika Nayl Al Rajaa Bi Sharh Safinat Al Najah.

Na pia kama alivyosema Shaykh U Islami Imam Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi kua: 'Wengi Miongoni mwa Wanazuoni ni wenye Mtizamo wa kua Haipendekezwi kufanya Istinjaa (Kukosha Tupu Mbili kwa Kutumia Maji) kutokana na Kulala usingizi, Kutokwa na Gesi, Kujigusa Utupu, Kugusana na Jinsia ya Mtu atakaekutoa Udhu.'*(Al Majmuu)*

Ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Imam Ibn Hajar Al Haytami katika *Tuhfah Al Muhtaj* na ndio Mtizamo wa Imam Al Shirbini katika *Al Mughni Al Muhtaj.*

Na pia amesema Imam Ali Al Shurunbulali Al Hanafi kua: **'Kufanya Istinjaa baada ya kutokwa na Gesi katika Utupu wa Nyuma hua ni Bidaa Potofu.'***(Imdad Al Fattah)*

Hivyo inapokua Tatizo si Gesi basi Mtu husika hua anatakiwa Afanue Istinjaa, na kisha ajaribu kutumia Kitambaa au Tissue ili kuzuia Najis hio isiingie kwenye Mavazi yake, kisha atatia Udhu hapo hapo bila kupoteza mda na Kuelekea kwenye sehemu ya Kusalia kwa ajili ya Sala. Hivyo kama ikiwa ataelekea Msikitini tuseme ni Katika Sala ya Jamaa au ya Ijumaa ambapo ndani yake mna Khutba ya Ijumaa basi ataruhusika kubakia na kusikiliza Khutba na kisha Kusali Sala ya Ijumaa.

Ambapo kusubiri kwake huko hakutohesabiwa kua ni Kusubiri kwani yeye hua hatakiwi kusubiri kwa hali ya Udhuru aliyokua nayo, na hivyo hata kama tuseme Tissue au Kitambaa kitaroa Damu au Matone ya Mkojo katika Kusubiri kwake basi Udhu wake hautokatika.

Na Sala yake itakua Sahih, ila sasa Kama itakua hali yake Ni mbaya sana kiasi ya kua Najis hio inachuruzika na kufikia kwenye Msala labda basi katika hali kama hii hua haruhusiki kuenda Msikitini kwa sababu ya kua atachafua sehemu za Kusalia hivyo mbali ya kua kwake hua

inakubalika lakini kwa wenzake haitokubalika Sala zao kutokana na Najis yake. Hivyo hua ni bora kwake kusali Nyumbani kwake.

Mtu Mwenye Hali ya Maadhur ataruhusika baada ya Kufanya Istinjaa na Kutia Udhu kusali, Kusoma Qur'an na hata kusali Sala za Sunnah katika Wakati wa Kipindi cha Sala husika ya Fardhi kaa Udhu huo huo alioanza nao lakini Udhu Huo Hubatilika mara tu anapomaliza Ibada yake ndani ya Kipindi hicho kwa maana hio, kikiingia kipindi chengine cha Sala basi atafanya kama alivyofanya katika Sala ya Kabla yake.

Mtu mwenye Hali ya Maadhur hua anapendekezwa Kusali Sala zake za Fardhi hadi Mwishoni mwa kipindi cha Sala husika, na hua haipendekezwi kwake kua Imam.

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ يُوسُفَ ، قَالَ : أَخْبَرَنَا مَالِكٌ ، عَنْ هِشَامِ بْنِ عُرْوَةَ ، عَنْ أَبِيهِ ، عَنْ عَائِشَةَ ، أَنَّهَا قَالَتْ : قَالَتْ فَاطِمَةُ بِنْتُ أَبِي حُبَيْشٍ لِرَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : يَا رَسُولَ اللَّهِ ، إِنِّي لَا أَطْهُرُ أَفَأَدَعُ الصَّلَاةَ ؟ فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : " إِنَّمَا ذَلِكِ عِرْقٌ وَلَيْسَ بِالْحَيْضَةِ ، فَإِذَا أَقْبَلَتِ الْحَيْضَةُ فَاتْرُكِي الصَّلَاةَ فَإِذَا ذَهَبَ قَدْرُهَا فَاغْسِلِي عَنْكِ الدَّمَ وَصَلِّي "

Amesema Abd Allah Ibn Yusuf kua amesema Imam Malik kua amesema Hisham Ibn Urwa kua amesema Baba yake (Ambae ni Urwa Ibn Zubayr kua amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua: 'Fatima Bint Hubaysh alimwambi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ya Rasul Allah! Hakika Mimi ni Mwanamke ambae kamwe siwi Tohara, Hivyo Jee Nisisali?

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Hio Ni Damu kutokana na Mshipa wa Damu na Si Damu ya Hedhi, Hivyo Utakapokua na Hedhi basi wacha Kusali, lakini Utakapomaliza Hedhi basi Ikoshe Damu hio na Usali.'(Sahih Bukhari)*

Ambapo hii ni Hadith Sahih ya Urwa Ibn Zubayr *Radhi Allahu Anhu* iliyonukuliwa zaidi ya mara 100 na Wanazuoni wa Hadith. Ambayo hutumika kama Kithibitisho cha Hukmu ya Maadhur yaani Mtu mwenye Udhuru wa kutokwa na Najis kutokana na kukosekana kwa uwezo wa Kuizuia isitoke na hivyo kukosekana uwezo wa Kuuthibiti Udhu wa Mhusika Usifisidike.

Na hali ya tatizo hili pia alikua nalo Imam Malik ambae ni Mwanzilishi wa Madhhab ya Imam Malik, ambae alikua na Tatizo la Kutoweza kuzuilika kwa Mkojo mwishoni mwa kipondi cha Uhai wake. Hivyo anasema Imam Ahmad Ad Dardir Al Maliki kua: **'Kama ikiwa Udhu utafisidika/utabatilika kutokana na kutokwa mara kwa mara kwa Mkojo bila ya kuzuilika basi hua unahesabika kua haubatiliki.'**

Ambapo Imam Al Dasuqi Al Maliki akafafanua Kauli hio ambayo ndio Kauli ya Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Madhhab mengineyo kama tutakavyoona hapo baadae In-shaa Allah kua: **'Maneno ya Ad Dardir kuhusiana na kua Kutokwa mara kwa mara kwa Mkojo bila Kuzuilika, hua kunajumuisha pia Tatizo la Kutokwa na Kinyesi, Gesi, Manii, Madhii, Madii n.k**

Ambapo Mtizamo aliouzungumzia Ad Dardir unahusiana na Mtizamo wa Watu wa Morroco wa Imam Malik ambao ni Mtizamo maarufu sana kaa upande wao Kwani kwa upande wa Watu wa

Baghdad ambao ni Wanazuoni wa Imam Abu Hanifa basi Wao wanasema kua hakuna Masharti ya mda wa Kutozuilika kwa Najis kunakobatilisha Udhu.

Hivyo Mtu hua anawajibika kutia Udhu kama ikiwa hali hio haikuendelea ndani ya Mda fulani lakini kama ikiwa hali hi ninya kuendelea basi Udhu hua haupendekezwi kutiwa kila Mara.'*(Hashiyah Al Dasuqi Al Maliki)*

Ambapo imesemwa kwenye *Mawsuah Fiqhiyyah Al Kuwaitiyyah* kua: Wanazuoni wote, isipokua wa Madhhab ya Imam Malik wanasema kua: '**Hua ni Wajibu kwa Mtu Mwenye hali ya Maadhur kutia Udhu mpya kwa ajili ya Kila Sala. Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanasema kua kwa Mtu mwenye kua na Hali ya Maadhur basi hua hana Ulazima wa Kutia Udhu ila hua Inapendekezwa Kutia Udhu. Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Imam Hanbal wanasema kua Mwenye Hali ya Maadhur hua anatakiwa kutia Udhu pale anapotaka Kusali katika Wakati wa Sala husika unapoingia.'***(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyyah)*

Kwani wa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi ili ahesbike kua ni Maadhur yaani mwenye Udhuru wa kukubalika Kisharia kutoweza kujidhibiti kutokana na Najis inayopelekea kufisidika kwa Udhu wake basi hua ni lazima kuwe na hali zifuatazo:

1-Tatizo hilo ni lazima liwe limo ndani ya Mda wote wa Sala,yaani Mtu husika kutokua na uwezo wa Kutia Udhu na kudumu nao bila kupata udhuru wa kubatilika kwa Udhu. Ambapo katika hali kama hii basi Hukumu yake ni kama ilivtokua katika Madhhab mengineyo ambayo ni kua humbidi kutia Udhu katika kila wakati anaposali, bila kujali kama utabatilika ama la.

2-Tatizo husika liwe ni la kudumu yaani ni lenye kuendelea kwa muda mrefu, ya kua ni mwemye kubatiliahika Ushu wake si chini ya mara mbili ndani ya kipindi husika cha Sala ambapo hii ndio itakayopelekea hali yake kujumuishwa kua ni miongoni mwa Maadhur.

3-Mtu mwenye Hali ya Maadhur hua ni mwenye kuhesabika kua ameshatoka kwenye hali hio. Pale itakapokua hatokewi na tatizo la kubatilika kwa Udhu wake ndani ya kipindi kizima cha Sala.'*(Imam Abu Ikhlas Ali Al Shurunbulali Al Hanafi katika Maraqi Al Saadat)*

Kisha Imam Al Shurunbulali anasema katika Nur Al Iddah kua: '**Kama ikiwa Mtu husika ametoka katika Hali ya kua Maadhur basi hua anatakiwa kuendelea na hukumu za Udhu kama vile ilivyokua kwa Waumini wengineo wa kawaida.**'*(Nur Al Iddah)*

Na akasema Imam Al Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: **'Kama ikiwa Mtu mwenye sifa ya Maadhur atatia Udhu na kabla ya wakati wa kuingia kwenye Sala na kisha akatokwa na kitu basi Udhu wake utafisidika.**

Kwa sababu ya Kua Udhu wake umebatilika katika wwakati wa kabla ya kuingia Wakati wa Sala. Na pia kwa sababu kukosa utohara humbatilishia Mtu Udhu. Lakini hali hii husameheaa na kutohesabiwapale inapokua hakuna uwezekano wa kujilinda ili Udhu ubatilike katika wakati ambao mtu anatakiwa kua tohara.

Hivyo kama akitia Udhu baada ya wakati huo (yaani katika wakati wa ndani ya kipindi cha Sala na akasali) basi Udhu wake utakubalika na atakua tohara na hatoathirika na kutokwa tena na udhu jambo ambalo halizuiliki kwake.'*(Al Mughni)*

Na akasema Imam Al Buhuti Al Hanbali kua: **‘Kama ikiwa Mtu atakua na hali ya Maadhur, iwe kutokana na Damu, Mkojo, Gesi, Madhii n.k.**

Basi anatakiwa kuikosha sehemu husika iliyochafuka kwa Najis husika na kisha ajiwekee pamba, kitambaa au Tissue, kwa ajili ya kuzuia kutoenea kwa Najis hio kwa kadri itakavyowezekana.

Na hatohitaika kurudia kujikosha na kujizuia Najis hio katika kila wakati wa kipindi cha Sala kama itakua amesahu, kwa sababu kwake yeye Najis hio hua hawezekani kuepukika hata afanye vipi.

Ila kutokana na hali hio basi hua ni Wajibu kwake kutia udhu katika kila wakati wa kipindi cha Sala kama akitokwana kitu.’*(Sharh Muntaha Al Iradah)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Sahnun Al Maliki basi yeye anasema kua: ‘**Hua haina haja ya Mtu mwenye sifa ya Maadhur Kujiwekea Kizuizi cha Kitambaa au Pamba, kwani kwake yeye kujisafisha kwa Maji tu hua kunatosheleza.’*(Mawahib Al Jalil)***

Na anasema Muhyi Ad Din Shaykh Ul Islami Ima. Abu Zakarriyah Sharaf Ibn Yahya An Nawawi Al Shafii kua: **‘Hukmu ya Al Bawl (Tatizo la Kutozuilika kwa Mkojo na Madhii) hua ni sawa na Hukmu ya Mwanamke mwenye Istihadhah, kama tulivyosema hapo Kabla.’**

Hukmu ya Mtu mwenye Tatizo la Fistula (Kua na Njia ya Haja Kubwa Pembeni ya njia ya Haja kubwa kunakosababishwa na kutoboka kwa njia ya haja Kubwa kutokana na Kidonda au Jeraha linalokuwepo pembeni yake kwa sababu tofauti) Bawasili au Kidonda Kinachotoka Damu katika Sehemu za Siri hua pia ni sawa na Hukmu ya Mwanamke mwenye Istihadha Kuhusiana na Kujisafisha Najis katika kila wakati wa kipindi cha Sala Kutokana na kua watu wenye Matatizo haya na kama haya hua hali ya kutokwa na Najis kila Wakati na hivyo hua ni kama hali ya Istihadha.’*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Imam An Nawawi anaendelea kutuambia kuhusiana na Mtu mwenye Tatizo la Kushindwa Kujizuia kutokana na Najis ya Mkojo, Manii, Madhii, Madii, Gesi, Kinyesi, Damu n.k kutozuilika kwa sababu ya Maradhi n.k kua: ‘**Wamesema As-habi Al Wujuh wetu(Wanazuoni Wakuu wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii) kua: Hukmu ya Tatizo la Mkojo na Madhii hua ni sawa na Hukmu ya Mwanamke Mwenye Istihadhah ambae hua na Wajibu wa Kujisafisha kwa Maji na kisha Kujiwekea Kitambaa, na Kutia Udhu kwa ajili ya Kila Sala ya Faradhi, na kuanza kwa kusali Sala ya Fardhi mara tu baada ya kutia Udhu huo.**

Ama kuhusiana na Fistula au Kidonda cha Sehemu ya Siri kinachotoka matone ya Damu, hua pia kama Hukumu ya Istihadhah kwa Mwanamke, kuhusiana na Kukosha Damu itokayo katika sehemu husika na kuweka Kitambaa kwa ajili ya kila Sala ya Fardhi.

Ambapo Udhu hua hauna ulazima pale inapokua Mtu ana hali ya Fistula au Jeraha isipokua pale itakapokua tatizo linatokana na ndani ya Tundu ya Haja kubwa ambayo ni katika hali itakayobatilisha Udhu’*(Al Majmuu)*

Imam An Nawawi anaendelea Kusema kua: **‘Hivyo kwa Mtu mwenye Tatizo la Mkojo, Kinyesi, au Gesi basi Hukmu yake pia hua ni sawa na Mwanamke mwenye Istihadhah katika kila kitu tulichokizungumzia juu yake, na As-hab Al Wujuh wetu wamekubaliana Juu ya hilo**

‘Ama kuhusiana Mtu anaetokwa na Manii tu kila wakati, basi Muandishi wa Al Hawi Al Kabir

(Imam Al Mawardi) amesema kua hua ni Lazima kwa Mtu huyo Kukoga Janaba katika Kila wakati wa Ibada ya Fardhi Na As-hab Al Wujuh wamesema kua Al Shafii amesema kua: Mtu mwenye Kutokwa na Manii mara kwa mara hua ni Dhaifu kwa sababu Kutokwa na Manii mara kwa mara hua kunasabisha upotezaji wa Uhai.'

Na Imam Al Baghawi aliulizwa kuhusiana na Mtu mwenye Tatizo la Mkojo katika hali ambayo akisimama basi Mkojo utamtoka lakini akikaa kitako basi Mkojo Huzuilika Jee asali vipi?'

Imam Al Baghawi akasema ama kuhusiana na hili basi kuna Mitizamo Miwili juu yake, na Mtizamo uliokua Sahih zaidi ni kua Bora Mtu huyo asali huku akiwa amekaa Kitako ili kuhifadhi Tohara ya Udhu wake, na hatokua na haja ya kuirudia Sala baada yake

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Qaffal Al Marwazi Al Shafii basi yeye amesema kua Mtu huyo itambidi tu Asali hukua akiwa Amesimama kutokana na kua anaweza kusimama.'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Naam hivyo katika Kuzungumzia kuhusiana na Salsal Al Bawl yaani Muendelezo kwa Kutokwa na Najis bila Kudhibitika kua Kihukumu hua ni sawasawa na hukmu ya Mwanamke anaetokwa na Damu ya Istihadha. Kuhusiana na Tohara yake, kwa sababu ya Dharurah yake na hivyo Maadhur au Mtu mwenye Dharurah husika hua anatakiwa kufahamu mambo yafuatayo:

1- Wajibu wa Sala ya Fardhi na Ibada nyenginezo hua hauondoki.

2-Kabla ya Kutia Udhu basi kwanza Inabidi Kujisafisha kutokana na Najis husika.

Na kisha Kuzuia muendelezo wa usambaaji wa Najis hio kwa kuweka Pamba, Kitambaa, Pampas n.k.

3-Kisha Kutia Udhu mara tu baada ya kutekeleza hayua mbili hizo za mwanzo yaani baada ya kujisafisha na kuizuia Najis husika.

Ambapo yote haya yanatakiwa kutekelezwa mara tu baada ya kuingia wakati wa Sala husika.

4-Hua ni Wajibu kutia Udhu kwa kufuata njia za Mfumo huu, ambapo ndani yake inaruhusika pia Kusali Sala na Sunnah na kufanya Ibada nyengine za Sunnah ndani ya wakati wa Ibada ya Sala husika.

5-Hua inapendekezwa Kucheleweshe kujitoharisha mara baada ya kuingia Sala husika ili kuweza kupunguza wingi wa Najis katika kipindi cha Sala husika.

Lakini hata hivyo hua hakuna madhara kama ikiwa mtu atachelewa Kufanya Ibada husika kwa sababu ya Maslahi ya kusikiliza Khutba ya Ijumaa kwa mfano, au kuchukua mda kufika Msikiti kutokana na Umbali wa Kimasafa, au Kusubiri Adhana, Au Iqamah au kufanya jitihada kwa ajili ya kutafuta Upande wa Kibla kwa aliekua mgeni wa Mji n.k.

Ambapo katika hali ya kusimamia Maslahi kama haya ya Kiibada basi Udhu wake hautotenguka hata kama ikiwa Najis hio Itapenya kutoka kwenye kizuizi alichotumia kama pamba kitambaa n.k.

6-Hivyo kama Maadhur akicheleweshа Sala bila ya kua na sababu maalum basi Udhu wake utabatilika,na hivyo itambidi aanze kujitoharisha Upya kwa kuanzia katika hatua ya kwanza ya Kujisafisha na Kunadilisha kizuizi.

7-Huwajibika Kusali katika Kila kipindi cha Sala kaa Udhu Mpya, tofauti na mtu mwemye kuweza kudumu na Udhu.

8-Huwajibika Kubadilisha Kizuizi hicho cha Pamba, Kitambaa,Tishu, Pampas n.k katika kila wakati anaotia Udhu.

9-Udhu wa Mtu mwenye hali ya Maadhur hua unabatilika pale atakapotokewa na Mambo mengineyo tofauti na tatizo lake yanayobatilisha Udhu.

Kwa Mfano Mtu husika ana ana tatizo la Mkojo, na akajitoharisha na kutia Udhu, lakini baada ya kutia Udhu akagusana na Mtu anaeweza kumtengua Udhu, au labda akatokwa na Gesi katika Utupu wa Nyuma, au akagusa Najis n.k basi Udhu wake utabatilika na hivyo kutakiwa kuanza tena hatua za Udhu kwa kulingana na Mfumo wa Udhu wa Maadhur tangu mwanzo hadi mwisho.

MUBTILAT SALAT – MAA'DHUR ALIEKOSA MAJI NA MCHANGA.

❖❖❖❖

Amesema Sultan Al Ulamaa Imam Abu Muhammad Izz Ad Din Ibn Abd Al Aziz Ibn Abd Salam Ibn Abi Qasim IBn Hasan Al Sulami Al Shafii kua: '**Yeyote yule aliekua na Jukumu la Kulitekeleza Kiwajibu kwa kufanya Utiifu, mbele ya (*Allah Subhanah wa Ta'ala*) Na akawa na uwezo wa kutekeleza baadhi ya sehemu ya jukumu hilo na sehemu nyengine akawa hawezi kutekeleza Basi na atekeleze lile atakaloweza, na lile asiloweza kulitekeleza hua hawajibiki kulitekeleza.'** *(Qawaid Al Ahkami)*

Na amesema Imam Ismail Al Bukhari kua:

عن عائشة رضي الله عنها: أنها استعارت من أسماء قلادة فهلكت فبعث رسول الله صلى الله عليه وسلم رجلا فوجدها فأدركتهم الصلاة وليس معهم ماء فصلوا فشكوا ذلك إلى رسول الله صلى الله عليه وسلم فأنزل الله آية التيمم فقال أسيد بن حضير رضي الله عنه لعائشة: "جزاك الله خيرا فوالله ما نزل بك أمر تكرهينه إلا جعل الله ذلك لك وللمسلمين فيه خيراً".

Amesema Ummu ul Muuminina Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: Aliazima Kidani kutoka kwa Asma na hivyo kikampotea na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamtuma Mtu akakitafute Kidani hicho. Na hivyo wakati wa Sala ukawafikia Watu hao lakini nao wakawa hawana Maji ya Kutilia Udhu, hivyo wakasali hivyo hivyo bila ya Udhu: Na kisha wakarudi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na kumlalamikia kuhusiana na Tukio hilo. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha Aya ya Tayammam.

Asid Ibn Hudayr *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: Allah akulipe kila la kheri, Wallahi, lolote lile litakalotokea ambalo hukulipenda basi Allah hua ni mwenye kulifanya Zuri kwa ajili yako na kwa Ajili ya Waumini.' *(Sahih Bukhari na Muslim)*

Naam..hii ni hadith ambayo imenukuliwa pia na Imam At Tabrani na pia na Abu Uwanah, Ambapo kwa upande wa Imam Bukhari basi ameiweka Hadith hii katika Kitabu chake katika Mlango usemao kua : **Kwa Mtu asiepata Maji wala Mchanga.'**

Na hivyo kulingana na Hadith hii basi tunaona kua inaruhusika kwa Mtu atakaekosa Maji au Mchanya wa kufanya Tayammam kusali bila ya Kutia Udhu, kwa sababu Mda wa Sala jmewadia kwake lakini njia ya Kutia Udhu hana. Na bila ya shaka hadith inatuonesha kua Tukio husika lilitokea kabla ya kushushwa Aya ya Udhu na amrisho la Kutayammam.

Na hivyo pia kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wanasema kua inapotokea hali kama hii ya Dharura basi hua inaruhusika Kusali bila ya Udhu. Au tuseme hali ya Mtu ambae ni Mgonjwa na hua hawezi kuyafikia Maji na wala hakuna mtu wa kumsaidia kutia Udhu. Au Mtu ambae yuko kifungoni na hana Maji ya kutilia Udhu,n.k

Na imesemwa katika Fat-h Al Barr kuhusiana na Hadith hii kua**: 'Amesema Ibn Rushd kua hii inatuonesha kama kwamba Imam Al Bukhari ameweka haki ya kutowezekana kwa Tayammam kutokana na kukosekana kwa mchanga. Yaani hii ni Hukmu ya kukosekana kwa vitoharishi viwili ambavyo ni Maji na Mchanga.**

Na hio ni kutokana na ufafanuzi wa Hadith hii uliowazi, kwa sababu Hadith haikusema kua Masahaba hao walikosa Mchanga, bali imesema kua walikosa Maji Hivyo hii inadhihirisha uthibitisho wa wajibu wa kusali kwa yule atakaekosa vitoharishi viwili hivi.

Na sababu ni kua wao Walisali kutokana na kuamini kua ni Wajibu wao, na kama ingekua imekatazwa basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angewakosoa, ambapo hivi ndivyo Imam Al Shafii, Imam Ahmad na Wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Hadith walivyosema.'*(Fat-h-al Barr)*

Ambapo amesema pia Imam Al Shawkani Al Hanbali kuhusiana na hadith hii kua: **Baadhi ya Wanazuoni wametumia Uthibitisho wa Hadith hii kuhusiana na kua Masahaba *Radhi Allahu Anhum* walisali bila ya Udhu kuthibitisha kua Sala hua ni Wajibu hata kama ikiwa kumekosekana Maji ya Kutilia Udhu na Mchanga wa kufanyia Tayamam. Ambapo Hadith hii haikuzungumzia kuhusiana na kukosekana kwa Mchanga bali kuhusiana na Maji tu, kwani kukosekana kwa maji katika wakati huo ilikua Ni Sawa na kukosekana kwa Maji na Mchanga, kwa sababu hakuna kitoharishi zaidi yake.**

Na hivyo Masahaba *Radhi Allah Anhum* walisali huku wakiamini kua Sala ni Wajib, hivyo kama ingekua imekatazwa hivyo basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angewakataza, na hivi ndivyo walivyosema Kina Al Shafii, Imam Ahmad, wafuasi wa Imam Malik na Wanazuoni wa Hadith.'*(Nayl Al Awtar)*

Na amesema Mansur Ibn Yusuf Al Buhuti Al Hanbali kua: '**Kama ikiwa Mtu hana Mkono, au amepooza Mwili n.k au anaumwa na hawezi kutia Udhu yeye mwenyewe basi inambidi atafute Mtu wa Kumtilisha Udhu, au Kumkogesha Janaba kwa kumsaidia au kwa kumlipa na hii ni kwa sababu Mtu husika hua ana jukumu Kiibada kama la Mtu mwenye Afya.**

Na kama ikiwa hakuna Mtu wa kumsaidia Kutia Udhu au Kufanya Tayamam na kwa sababu hana uwezo wa Kumlipa Mtu basi itambidi Mtu Mtu huyo kusali katika hali aliyokua nayo.'*(Kashshaf Al Qina)*

Na akasema Imam Ibn Al Qayyim Al Jawziyyah Al Hanbali kua: '**Hali ya kutokua na Maji hua ni sawa na hali ya kutokua na Mchanga tohara na hakuna utofauti juu yake. Na Masahaba hawa *Radhi Allahu Anhum* Walisali bila Tayammam kwa sababu Tayammum ilikua haijaruhusiwa**. **Ambapo hii hua ni sawa na Mtu atakaesali bila kufanya Tayammam kwa sababu ya kukosa Mchanga wa kufanyia Tayammam.**

Hivyo jee kuna tofauti gani baina ya kutokua na Mchanga na kutoruhusika kutumia mchanga? Hivyo hapa yametumika Matumizi ya Makisio ya Kiasi na Sunnah kua Mtu anatakiwa asali kulingana na hali ya mazingira aliyokua nayo.

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* haibebeshi Nafsi zaidi ya isichokiweza, na hivyo Mtu hatotakiwa kuirudia Sala hio, kwa sababu ameshatekeleza kile alichoamrishwa, hivyo haina haja kwake kukirudia Hivyo hii hua ni sawa na Mtu asieweza Kusimama, asieweza kuelekea Kibla, asieweza kukabiliana na Sutra, na asieweza kusoma Qur'an ndani ya Sala kwa sababu hajui kusoma, Hivyo hii ni kulingana na Makisio na Sunnah.'*(Tahdhib Sunnan Abi Daud)***

Na kwa upande wa Muwwafaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali basi yeye anasema kua: '**Ama kuhusiana na mtizamo nimaoupendelea mimi zaidi juu ya hili ni kua kwa asieweza kujitoharisha kwa maji wala mchanga Basi na asali katika hali aliyokua nayo na hatowajibika kuirudia Sala yake hio hata kama hapo baadae atapata Maji.**

Ambapo huu ndio pia Mtizamo wa Imam Al Shafii, Imam Abu Hanifa na Imam Al Thawry. **Ama kwa upande wa Imam Al Awzai basi yeye anasema kua Mtu husika hatakiwi kusali hadi atakapopata Maji, na kisha alipe Sala hio kwa sababu Sala ni Ibada ambayo haifutiki wajibu wake wa kuitekelezwa, hivyo sio lazima Kusali kwani atalipa kama ilivyokua Funga kwa Mwanamke mwenye Hedhi.**

Ambapo kwa Upande wa Imam Malik basi amesema kua Mtu atakaekosa Maji na Mchanga basi asisali na wala hatowajibika kuilipa kwa sababu ya kua amekosa Kitoharishi, na hivyo Sala haitokua Wajibu kwake kama kwa Mwanamke mwenye Hedhi.

Na Imam Ibn Abd Al Barr amesema kua: "Hii ni kauli ngeni sana kutoka kwa Imam Malik" Na kisha Imam Ibn Abd Al Barr akanukuu mitizamo Miwili ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik ambapo Mmoja miongoni mwao ni kama wa Imam Abu Hanifa na kisha wa pili ni usemao kua Mtu husika atasali katika hali aliyokua nayo, lakini baadae atarudia Sala hio.

Kwani Hadith inaonesha kua Udhu haikua Wajibu, bali ni Sharti hivyo Sala hua haitakiwi kucheleweshawa pale unapokosekana Udhu,kama vile inavyokua Mtu hajui Upande wa Kibla. **Hivyo kwa uthibitisho huu basi kama Mtu atasali katika hali aliyokua nayo, na kisha akakutana na Maji au Mchanga Tohara basi hua hatakiwi kuirudia Sala hio aliyokwishaisali.**

Na hii ni kulingana na Mtizamo mmoja kati ya Miwili juu yake, ambapo katika mtizamo wa pili hua ni kua Kuna Ulazima wa Kuirudia Sala husika ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Al Shafii, na hii ni kwa sababu Sala ya Mtu husika hua imevunja Sharti la Sala ambalo ni la Kusali Bila kua Tohara.

Ambapo Mtizamo wa kwanza ndio Sahih kulingana na Hadith husika, kwa Masahaba hao walifanya waliyoamrishwa na hivyo wameshaondokana na Jukumu la amrisho husika, na kuhusiana na Sharti la Sala basi hua halitIliwi maanani kwa sababu halitekelezeki. Na pia

Masahaba hawa *Radhi Allahu Anhum* wamejitahid kwa kadiri ya uwezo wao wa juu kabisa, hivyo haina haja kurudia Sala, kama vile ambavyo Mtu atakapokosa Nguo na ikambidi Asali bila ya Nguo, au asiejua upande wa Kibla, au asiweza kusimama.*'(Al Mughni)*

Na akasema Shaykh Ul Islami Imam Anu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi al Shafii kua: **'Kama Muislam atashindwa kutia Udhu yeye mwenyewe basi anatakiwa atafute Mtu wa kumsaidia iwe kwa bure au kwa malipo. Na kama haitowezekana hivyo basi Muislam huyo atatakiwa kusali katika Hali aliyokua nayo ambayo itakua na wepesi kwake. Hivyo Kama Muislam akikosa Maji ya Kutilia Udhu na akakosa Udongo msafi au Kokoto kwa Tayammam, basi inambidi asali Saala yake hivyo hivyo katika mazingira aliyokua nayo ndani ya wakati wa Sala unapoingia, lakini itambidi airudie Sala atakapopata Maji au Udongo Tohara, kwa sababu Sala hua ina kasoro inapokua haijatiliwa Udhu'***(Al Majmuu)***

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Ama kuhusiana na Hukmu ya Mtu aliekosa Maji na Mchanga wa Kujitoharishia kwa ajili ya Kutilia Udhu, labda kwa sababu amekwama kwenye Matope au kwenye sehemu isiyokua Tohara na ameshindwa kupata Maji ya Kujitoharishia au kitu kama hicho basi kuna mitizamo minne juu yake katika Skuli yetu.**

Ambapo Mtizamo wa kwanza ni Mtizamo wa Wanazuoni wetu wa Khurasan ambao wamesema kua: 'Mtu huyo atatakiwa Kusali pale utakapoingia wakati wa Sala katika hali na mazingira aliyokua nayo, ambapo hata hivyo kama akifanikiwa kupata Maji au Mchanga hapo baadae atakapotoka kwenye Mazingira hayo basi itambidi kuilipa Sala hio ambao huu ndio Mtizamo sahih ambao wengi miongoni mwa Wanazuoni wetu wamekubaliana nao kutokana na vithibitisho vyenye nguvu.

Mtizamo wa pili ni ule usemao kua kama ikiwa Mtu atajikuta katika hali kama hii basi hua hakuna Wajibu kwake Kusali, bali kuna pendekezo tu kua Asali katika hali aliyokua nayo na kisha pia alipe baadae iwe ameisali sala hio ama la, ambapo huu ni Mtizamo wa Shaykh Abu Hamid na Wanazuoni wetu wa Iraq.

Mtizamo wa Tatu kuhusiana na Mtu atakaejikuta katika Mazingira ya kukosa Maji na Mchanga kwa ajili ya kutilia Udhu basi ni Kua Hairuhusiki kwake Kusali, hivyo itambidi baadae atakapopata Maji au Mchanga itambidi kuilipa Sala hio, ambapo huu ni Mtizamo wa Imam Al Haramayn na baadhi ya Wanazuoni wa Khurasan kutoka katika Kauli ya Zamani ya Madhhab ya Imam Al Shafii *yaani Al Qawl Al Qadim.*

Na Mtizamo wa Nne kuhusiana na Mtu mwenye hali ya mazingira Kama haya ya kukosa Maji na Mchanga pia kwa Kutilia Udhu basi ni Kua Sala hua ni Wajibu kwa Mtu pale utakapoingia Wakati wake, hivyo humbidi Mtu kuisali Sala katika Wakati wake kwa haki yeyote ile atakayokua nayo, kulingana na mazingira yake na kisha hatowajibika kuilipa Sala hio ambapo huu pia ni Mtizamo wa Al *Qawl Al Qadim.*

Ambapo anasema Imam Al Haramayn kuhusiana na uthibitisho wa kauli hizi kua: Kama tukisema kua Sala hua ni Wajibu kuisali katika wakati wake, na ni Wajibu kuilipa, basi knachobainika katika Madhhab yetu hua ni kua kile kilichotekelezwa kwenye wakati wake hua ni Sala, lakini hata hivyo kutokana na kua na Kasoro ya kukosekana kwa Udhu basi hua inabidi kurudia Sala husika kwa ajili ya kuikamilisha Sala husika.'*(Al Majmuu Sharh Al Muhaddhab)***

Imam An Nawawi anaendelea kutufafanulia zaidi kua: '**Kulingana na Madhhab yetu basi kama Ikiwa Mtu husika aliejikuta kwenye Mazingira kama haya ya kukosa Maji na kukosa Mchanga, na hivyo akasali, na baada ya kufunga Sala akaona Maji mbele yake au Mchanga, basi Sala yake hio Utabatilika hapo hapo, ambapo huu ndio Mtizamo Sahih na ndio Mtizamo Unaotegemewa na wengi miongoji mwa Wanazuoni wetu, mbali ya kua pia kuna Mtizamo wa Qadhi Hussein aliesema kua Sala hio haitobatilika ambao ni kama Mtizamo wa Tariqah ya Khurasan.'***(Al Majmu Sharh Al Muhadhdhab)***

Naam..tumeona Mtizamo wa Wanazuoni kuhusiana na kukubalika kwa Maadhur yaani mtu mwenye kua na Dharurah kuruhusika Kusali bila ya Udhu pale atakapokua ana dharurah ya kutoweza kupata Maji au Mchanga kwa ajili ya kujitoharisha na Wakati wa Sala ya Fardhi umeshaingia,kulingana na Mitizamo ya Madhhab tofauti.

Mbali ya kua kuna hadith isemayo kua: Amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua, amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*: *Allah Subhanah wa Ta'ala* haikubali Sala ya Mtu ambae hana Udhu.'*(Sahih Muslim)***

Na zikaamrisha aya za Qur'an kwa kusema kua:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقۡرَبُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنتُمۡ سُكَٰرَىٰ حَتَّىٰ تَعۡلَمُواْ مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغۡتَسِلُواْۚ وَإِن كُنتُم مَّرۡضَىٰٓ أَوۡ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوۡ جَآءَ أَحَدٞ مِّنكُم مِّنَ ٱلۡغَآئِطِ أَوۡ لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمۡ تَجِدُواْ مَآءٗ فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدٗا طَيِّبٗا فَٱمۡسَحُواْ بِوُجُوهِكُمۡ وَأَيۡدِيكُمۡۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَفُوّٗا غَفُورٗا﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo la taqraboo alssalata waantum sukara hatta taAAlamoo ma taqooloona wala junuban illa AAabiree sabeelin hatta taghtasiloo wa-in kuntum marda aw AAala safarin aw jaa ahadun minkum mina algha-iti aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban faimsahoo biwujoohikum waaydeekum inna Allaha kana AAafuwwan ghafooran. *(Surat An Nisaa 4: 43).*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Msiikaribie Sala wakati mkiwa mmelewa hadi pale mtakapojua maana ya mkisemacho, wala mkiwa katika hali ya janaba isipokua pale mtakapokua safarini (bila ya kua na maji ya kutosha), hadi mtakapokosha mwili wenu wote. Na mkiwa mnaumwa, au mko safarini au mnapoenda haja au mnapo wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi, kupangusa nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Allah ni mwingi wa kusamehe na msamehevu sana'.***

Na ikasema hadit ifuatayo kua:

حَدَّثَنَا سُوَيْدُ بْنُ سَعِيدٍ، حَدَّثَنَا عَلِيُّ بْنُ مُسْهِرٍ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ، طَرِيفٍ السَّعْدِيِّ ح وَحَدَّثَنَا أَبُو كُرَيْبٍ، مُحَمَّدُ بْنُ الْعَلاَءِ حَدَّثَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، عَنْ أَبِي سُفْيَانَ السَّعْدِيِّ، عَنْ أَبِي نَضْرَةَ، عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ، عَنِ النَّبِيِّ ـ صلى الله عليه وسلم ـ قَالَ " مِفْتَاحُ الصَّلاَةِ الطُّهُورُ وَتَحْرِيمُهَا التَّكْبِيرُ وَتَحْلِيلُهَا التَّسْلِيمُ

Amesema Suwaidu Ibn Said kua amesema Aliyyu Ibn Mus-hir kua amesema Abi Sufyan kua amesema Taririf Ibn Saidi kua amesema Abi Nadhrat kua amesema Abu Said Al Khudhri *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua Ufunguo wa Sala ni Udhu, Kuingia ndani yake ni kwa Allahu Akbar na kuifunga kwake ni kwa Salam.'*(Sunnan At Tirmidhii, Sunnan Abu Daud,Musnad Imam Ahmad)***

Ambapo Aya na Hadith hizi ni zenye Kukataza Kusali bila ya kua na Udhu.

Na hivyo baadhi ya Wanazuoni kutoa mfano wa kua Mtu Mwenye Hali ya kutokua na uwezo wa kupata Maji Tohara au Mchanga Msafi basi hua ni mwenye kua katika hali Sawia na hali ya Mwanammke mwenye Hedhi ambae hua haruhusiki Kusali hadi itakapokoma Hedhi yake.

Kwani Mtu husika hua si Tohara kutokana na Kukosa Udhu na kukosa njia za vyanzo ya Kujitoharishia kwa ajili ya Ibada ya Sala.

Ambapo kwa upande mwengine kama tulivyoona kua wengi miongoni mwa Wanazuoni ni wenye kupingana na Mtizamo huo na hii ni Kulingana na uthibitisho wa Hadith tuliyoelezea isemayo:

عن عائشة رضي الله عنها: أنها استعارت من أسماء قلادة فهلكت فبعث رسول الله صلى الله عليه وسلم رجلا فوجدها فأدركتهم الصلاة وليس معهم ماء فصلوا فشكوا ذلك إلى رسول الله صلى الله عليه وسلم فأنزل الله آية التيمم فقال أسيد بن حضير رضي الله عنه لعائشة: "جزاك الله خيرا فوالله ما نزل بك أمر تكرهينه إلا جعل الله ذلك لك وللمسلمين فيه خيراً".

Amesema Ummu ul Muuminina Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: Aliazima Kidani kutoka kwa Asma na hivyo kikampotea na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamtuma Mtu akakitafute Kidani hicho. Na hivyo wakati wa Sala ukawafikia Watu hao lakini nao wakawa hawana Maji ya Kutilia Udhu, hivyo wakasali hivyo hivyo bila ya Udhu: Na kisha wakarudi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na kumlalamikia kuhusiana na Tukio hilo. Hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha Aya ya Tayammam.

Asid Ibn Hudayr *Radhi Allahu Anhu* akasema kumwambia Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: Allah akulipe kila la kheri, Wallahi, lolote lile litakalotokea ambalo hukulipenda basi Allah hua ni mwenye kulifanya Zuri kwa ajili yako na kwa Ajili ya Waumini.'*(Sahih Bukhari na Muslim)***

Na hivyo wenye Kuunga Mkono kuruhusika Kusali bila ya Udhu katika wakati wa Dharurah wa kukosa Maji au Mchanga tohara wanasema kua: Ushahidi wa Hadith hii unaonesha kua Watu haaa walisali bila ya kua Tohara na *Rasul Allah Salallhu Alayhi wa Salam* hakuwaambia watu hao warudie Sala hio, kwa sababu kuamrishwa kurudia Sala hio hua ni sawa na kusali Sala Moja mara mbili katika Siku Moja.

Na kusali kwa Masahaba hawa hua ni sawia na kuruhusika Kusali kwa Mwanammke mwenyr Istihadhah, au Mtu asiekua na Nguo, au Atakaesali kwa Kuashiria kutokana na Kuumwa sana au kutokana na Khofu ya kuonekana na Maadui zake.

Hivyo Masahaba haaa walisali kutokana na kujua kua Kuisali Sala katika Wake hua ni Wajibu, nao Wakasali kulingana na Mazingira ya hali waliyokua nayo, na walimwambia *Rasul Allah*

Salallahu Alayhi wa Salam **ambapo nae hakusema kua Sala hua si wajibu katika Mazingira kama haya Na Kama ingekua Si Wajibu basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angewabainishia wazi kama vile alivyombainishia Amar ibn Yasir *Radhi Allahu Anhu* alipomwambia kua:**

Ingekutosheleza wewe kama ungefanya kadhaa wa kadhaa, na pia kulingana na hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* ambayo amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Chohote kile nilicho kukatazeni basi achaneni nacho na nilichokuamrisheni basi kifanyeni sana kwa kadri Mtakavyoweza*(Imam Muslim)***

Hivyo Imam An Nawawi anasema kua: Amesema Imam Al Abu Al Abbas Al Jurjani katika Al Muayah kua: Hakuna Kuingia ndani ya Sala ya Fardhi bila ya Udhu kunakokubalika, au Sala ya Sunna Bila ya Udhu kunakokubalika Isipokua kwa Yule Mtu ambae amekosa Maji na amekosa Mchanga Msafi au Mwenye Najis ambayo kamwe hawezi kujiepusha nayo.

Hivyo hata kama ikiwa Mtu atakua amefungwa na maadui zake kwa Minyororo iliyomkaza kwenye Kiguzo,au Mfungwa, au kua kwa Mtu anaekuzuia Kusali, basi Mtu husika hua anatakiwa kusali kwa kulingana na hali aliyokua Nayo.'(*Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

MUBTILAT SALAT- MA'ADHUR MWENYE MFUKO WA MKOJO

❖❖❖❖

Naam baada ya kuangalia kuhusiana na hali ya Mazingira ya Sala y Maadhur ya Mtu asiekua na Maji au Mchanga Mkavu kwa ajili ya Udhu na Kutayamam kwa ajili ya Ibada ya Sala.

Basi na tuangalia kuhusiana na Udhu na Sala ya Maadhur mwengine ambae ni Mtu mwenye Tatizo la Mkojo, yaani kwa mfano Mkojo kuziba na hivyo kutiwa Mpira wa Mkojo.

Ambao hua unaunganishwa na Mfuko wa Kukusanyia Mkojo kutoka ndani ya Kibofu cha Mkojo hadi nje ya mwili wake na hivyo Mtu huyo kua aidha yuko kitandani na Mfuko wake au anatembea na Mfuko wake huo wa Mkojo iwe Mwanamme au Mwanamke.

Ambapo hili pia ni jambo la Dharurah lenye kuwatokezea wengi sana siku hizi miongoni mwa Watu Wazima Wanaume kwa sababu ya Matatizo ya maradhi ya Tezi Dume.

Ambapo kwanza Kwa Maadhur mwenye Dharurah kama hii basi hua ni sawa na Mtu mwenye kushindwa kuudhibiti Mkojo, Au Choo Kikubwa au Damu kutoka katika Tupu mbili kihukmu kulingana na Udhu wake.

Na hivyo basi kama tulivyosema hapo kabla kua inabidi kujitoharisha pale unapoingia wakati wa Sala husika, kisha kutafuta kitu cha kuzuia Najis husika kama Kitambaa, Pamba au Tissue kisha kutia Udhu na Kusali kabla ya kupita wakati wa Sala husika. Na kutakiwa kufanya hivyo katika Kila kipindi cha Sala.

Na ingawa haoi zao hua zinafana wenye Dharurah hii ya kutiwa Mpira na wasiotiwa Mpira ila sasa tofauti inayojitokeza baina ya Mtu mwenye Kubeba Mfuko wa Mkojo hua ni mwenye Kubeba Najis hio ndani ya Mfuko. Na hivyo Wanazuoni wametofautiana juu ya Hukmu inayohusiana na hali ya Dharurah hii.

Kwani anasema Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shirbini Al Khatib Al Shafii kua:

Sala ya Mtu Mwenye Kubeba Najis kwenye Mvazi yake hua ni Batili, kwa sababu Sharia hua inamtaka Mtu anaefanya Ibada kua ni Tohara Kimwili na Kimavazi, na hivyo kubeba Najis hua Kunapingana na Utohara huo unaotakiwa Kisharia.'*(Al Mughni Al Muhtaj)*

Kwa maana hio basi mtu mwenye Dharurah kama hii hua anatakiwa afuate Hukumu ya Mtu mwenye Dharurah ya kutoweza kuzuia Najis, na hivyo atatakiwa kuifungua Chupa husika ya Mkojo au Najis husika na kisha Kuisafisha kutokana na Najis husika, kisha kuifunga Upya kwenye Mpira wake kabla ya Kutia Udhu na Kusali kama tulivyosema hapo awali.

Ambapo hii itakua na sawa na Mtu ambae Mwenye kutakiwa kubadilisha Kitambaa au Pamba.

Na hali tunazungumzia kwa Mtu ambae anao uwezo wa Kuifungua Chupa hio na Kuisafisha, lakini kama itakua Mtu husika hana uwezo huo na haiwezekani, au akifanya hivyo basi atajisababishia Madhara, au labda Kidaktari hua haikubaliki, au Mfuko huo hausafishiki n.k.

Basi bila ya Shaka hapa itabidi itumike njia nyengine ya kupitia kwenye Kanuni ya Fiqh isemayo kua *Al Mashaqat Tajlib Al Taysir* - Mashaka Huleta Wepesi. Na hivyo basi Mtu husika ataruhusika Kusali katika Hali aliyokua nayo.

Ila sasa kwa Upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao Wanasema kua Kwa Mtu mwenye Hali kama hii basi itambidi Asali katika hali aliyokua nayo na kisha akishatolewa Mpira basi atatakiwa alipe Sala zote alizosizali katika wakati alipokua na Mpira huo, ambapo huu ndio Mtizamo unaotegemewa na kukubalika zaidi katika Madhhab.

Kwani anasema Shaykh ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Kama Mtu akichukua Yai ambalo nje yake itakua ni Safi lakini ndani yake mna Damu, au akichukua Shada la Zabibu ambalo ndani yake limekua ni Mvinyo na haujachuruzika nje, na kisha akasali basi Sala yake itakua Batili. Na hii ni kulingana na Mtizamo unaokubalika zaidi, ambapo Mifano hii miwli inazungumzia Kizuizi cha Kimaumbile cha Vitu viwili hivi ambavyo hata hivyo vimebebea Najis.**

Hivyo kama Mtu akichukua Chupa ambayo Ufuniko wake ni wa Fedha au mitihili yake, na chupa hio ndani yake ikawa imebeba Najis, na kisha Mtu huyo akasali basi Sala ya Mtu huyo itakua Batili, na hivyo hata kama chupa hio ataizungushia Tambara, basi Sala yake itakua Batili pia. Na hata kama Mtu akibeba Nyama ya Mnyama baada ya Kumchinja na kumsafisha na kisha akasali huku akiwa amebeba Mnyama huyo basi Sala yake hua ni Batili.'*(Rawdhat At Talibin wa Umdat Al Muftin)*

Hivyo huo ni ufafanuzi wa baadhi ya vitu ambavyo vitapelekea Sala ya Mtu husika Kubatilka, na tunapoangalia mifano ya vitu hivi basi tunaona kua ndani pia mnaingia kitu tunachokizungumzia katika Mada yetu ambacho ni Mfuko wa Mkojo.

Na amesema Al Muhaqqiq Imam Ibn Aabidin Ash Shami Al Hanafi kua; **'Kama ikiwa Mtu atabeba Chupa ambayo ina mkojo ndani yake huku ikiwa imezibwa kwa kifuniko kilichokaza sana, basi Sala yake Mtu huyo haiyokua ni sahih bali itakua ni Batili.**'*(Radd Al Muhtar)*

Na Muwwafaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdiai Al Hanbali kua**: 'Kama ikiwa Mtu atabeba Chupa ambayo ni yenye kubeba Najis ambao umefungiwa Ndani yake basi Sala ya Mtu huyo itakua ni Batili.'***(Al Mughni)*

Na Imam Al Mardawi Al Hanbal kua: **'Kama Mtu atabeba Chupa ambayo ni yenye kua na Najis ndani yake au Kitofali cha kuoka kwa Moto ambacho ndani yake kina Najis, basi Sala ya Mtu huyo itakua Batili.**'*(Al Insaaf)*

Na kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi anasema Imam Al Khurashi Al Maliki kua: '**Kama ikiwa Mtu amesali huku akiwa amebebea Mfuko wa Najis kwa sababu ya kutoweza, kuutoa au kutoweza kuimwaga Najis hio na kuusafisha mfuko huo basi Mtu hua inapendekezwa kwake azirudie zile Sala ambazo zimeendana sambamba kiwakati na mda ambao imewezekana Kuutoa au kuusafisha Mfuko huo.**'*(Mukhtasar Al Khalil)*

Na miongoni mwa Masuali basi ni kua: '**Hivi Jee inaruhusika kwa Maadhur yaani Mtu mwenye Udhuru wa kutoweza kukaa na Udhu kua Imam?'**

Ambapo juu ya Jambo hili basi Wanazuoni wanakubaliana kua: Inakubalika kwa Maadhur Mwenye Kua na Udhuru wa Kutoweza kukaa na Udhu kua Imam kwa ajili ya Maamuma ambae ni Maadhur Mwenzake.

Na tunapoangalia kuhusiana na Maadhur kua Imam mbele Mtu asiekua na Tatizo hilo kiafya basi Wanazuoni wametofautiana Juu yake kwani Imesemwa kwenye Mawsuah Al Fiqhiyyah Al Kuwautiyyah kua: **'Wanazuoni wanakubaliana kua Sala ya Maadhur atakaeku Imam mbele ya Maamuma ambae ni Maadhur Mwenzake basi hua Inasihi.**

Lakini kwa upande wa Sala ya Imam Maadhur mbele ya Maamuma mwenye Afya yake basi kuna kutofautiana baina ya Wanazuoni na hivyo kuna mitizamo miwili juu yake ambayo ni:

1-Kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wao wana Mtizamo usemao kua: Haikubaliki kwa Maadhur Kumuongoza asiekua Maadhur Katika Sala, kwa sababu wale wenye hali ya kua ni Maadhur hua ni wenye Kuruhusika Kusali huku wakiwa na Najis kutokana na hali yao na hivyo Najis hio huchukuliwa kua kama haipo kwao wao, kutokana na kuhitajika kwao kutekeleza Majukumu yao Kiibada.

Hivyo hii hua ni hali ya dharurah ambayo hua inaruhusika kwa ajili yao wao tu, na hivyo basi wao hua ndani ya mipaka ambayo haitakiwi kuvukwa lakini wameivuka kutokana na Udhuru wao.

Hivyo Mtu mwenye Afya yake hua na hali bora na yenye nguvu zaidi kutokana na kua hakuvuka mipaka husika,kuliko Maadhur Na kutokana na kua na hali hio basi Mtu mwenye Afya ndio anagakiwa amuongoze mwenye hali ya Maadhur na wala sio kinyume chake.

2-Ama kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua: 'Inaruhusika kwa Maadhur kumuongoza Mtu mwenye Afya katika Sala, kwa sababu Sala ya Maadhur wasiotakiwa kuirudia Sala yao basi hua Sahih kwa sababu wameruhusika kusali kutokana na Udhuru waliokua Nao Na hivyo hii inajumuisha pia katika kuongoza na kufuatwa katika Sala pia.

3-Kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: Ingawa hua inaruhusika kwa Maadhur kua Imam mbele ya Maamuma mwenye Afya lakini hata hivyo hua ni Makruh.' *(Mawsuah Al Fiqhiyyah Kuwaytiyyah)*

Ambapo Mtizamo wa kwanza ni kama alivyosema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi kua: **'Sala ya Mwanammke mwenye Istihadhah, Sala ya Mtu Mwenye Matatizo ya Mkojo n.k hua ni Sala Sahih na inayokubalika kwa Watu husika tu na watu wenye Matatizo kama hayo. Na hivyo Sala hio hua ni Batili kwa Mtu mwegineo asiekua Maadhur kwa sababu hua ni Sala iliyovunja Sharti la Sala. Na hivyo hua ni sawa na Sala ya Mtu alielala kua Imam kwa Mtu mwenye afya yake na Kusimama.**' *(Al Kafi*)

Na akasema Imam Al Buhuti Al Hanbali kua: '**Sala ya Mtu mwenye Afya yake Nyuma ya Maadhur mwenye tatizo la Mkojo, Gesi, Damu ya Pua isiyokata,Jeraha linalotiririka Damu n.k hua ni Batili. Kwa sababu Sala ya Maadhur hua ina kasoro ambayo hairekebishiki, kutokana na Najis inayomtoka ambayo haimfanyi kua Tohara, Hivyo Sala ya Maadhur hua ni Sala inayokubalika kwa ajili yake mwenyewe kutokana na Dharurah aliyokua nayo.'** *(Kashshaf Al Qinaa)*

Na kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii basi amesema kua: '**Inaruhusika kwa Maadhur wa Kiume kua Imam na Kufuatawa na Maamuma ambae ni Mzima mwenye afya yake, na pia inaruhusika kwa Mwanammke mwenye Istihadhah kua Imamat kwa Mwanamke mwenzake Mwenye Afya yake.**'*(Rawdhat Talibin)*

Na akasema tena Imam An Nawawi katika *Matn Al Minhaj* kua: '**Mtizamo uliokua sahih zaidi ni kua inaruhusika kwa Mtu mwenye Afya yake kua Maamuma nyuma ya Mtu mwenye Tatizo la Mkojo.'***(Matn Al Minhaj)*

Na katika Al Majmuu tunaona kua Imam An Nawawi anaendelea kuasema kua: **'Mtizamo unaokubalika Zaidi katika Madhhab yetu ni kua Sala ya Maamuma mwenye Afya nyuma ya Imam Ambae ni Maadhur hua inasihi, na huu ndio pia Mtizam wa Imam Al Haramayn na Imam Al Ghazali katika Al Basit, ambapo Wanazuoni wamechukua makisio ya Mtu anefanya Istinjaa au watu ambao wamesamehewa Najis yao katika Miili yao au Nguo zao.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na amesema Imam Ibrahim Ibn Abd Al Aziz Al Dasuqi Al Maliki kua: **'Inaruhusika kwa Mtu mwenye Afya yake kua Maamuma mbele ya Maadhur, lakini hua ni Makruh.'***(Khashiyah Al Dasuqi)*

MUBTILAT SALAT – MAA'DHUR MWENYE BENDEJ AU PLASTA

❖❖❖❖

كُسِر زندي يوم أحد فسقط اللواء من يدي، فقال النبي صلى الله عليه وآله وسلم: «اجْعَلُوهَا فِي " يسَاره فَإِنَّهُ صَاحب لِوَائِي فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَة»، فقلت: يا رسول الله ما أصنع بالجبائر؟ فقال: «امْسَح عَلَيْهَا»

Anasema Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Sehemu ya mwishoni mwa Mkono wangu ilikua kimevunjika, katika Vita vya Uhud, na hivyo Bendera Ikanianguka kutoka Mkononi mwangu. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam akasema kuwaambia Masahaba,

Muwekeeni Bendera katika Mkono wake wa Kushoto, kwa sababu yeye ndie mbebaji wa Bendera yangu hapa Duniani na Akhera pia.

Hivyo nami nikasema: Ya Rasul Allah Jee nifanyeje kuhusiana na Bendeji yangu?.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam akasema, Utapaka Maji Juu yake.'*(Musannaf Ibn Abd Razzaq, Sunnan Ibn Majah, n Sunnan Al Kubra Imam Al Bayhaqi)*

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua:

حَدَّثَنَا مُوسَى بْنُ عَبْدِ الرَّحْمَنِ الأَنْطَاكِيُّ، حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ سَلَمَةَ، عَنِ الزُّبَيْرِ بْنِ خُرَيْقٍ، عَنْ عَطَاءٍ، عَنْ جَابِرٍ، قَالَ خَرَجْنَا فِي سَفَرٍ فَأَصَابَ رَجُلاً مِنَّا حَجَرٌ فَشَجَّهُ فِي رَأْسِهِ ثُمَّ احْتَلَمَ فَسَأَلَ أَصْحَابَهُ فَقَالَ هَلْ تَجِدُونَ لِي رُخْصَةً فِي التَّيَمُّمِ فَقَالُوا مَا نَجِدُ لَكَ رُخْصَةً وَأَنْتَ تَقْدِرُ عَلَى الْمَاءِ فَاغْتَسَلَ فَمَاتَ فَلَمَّا قَدِمْنَا عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم أُخْبِرَ بِذَلِكَ فَقَالَ " قَتَلُوهُ قَتَلَهُمُ اللَّهُ أَلاَّ سَأَلُوا إِذْ لَمْ يَعْلَمُوا فَإِنَّمَا شِفَاءُ الْعِيِّ السُّؤَالُ إِنَّمَا كَانَ يَكْفِيهِ أَنْ يَتَيَمَّمَ وَيَعْصِرَ " . أَوْ " يَعْصِبَ " . شَكَّ مُوسَى " عَلَى جُرْحِهِ خِرْقَةً ثُمَّ يَمْسَحَ عَلَيْهَا وَيَغْسِلَ سَائِرَ جَسَدِهِ " .

Amesema Musa Ibn Abd Rahman Al Antaky kua amesema Muhammad Ibn Salamat kua amesema Zubayr Ibn Khuraqi kua amesema A'ta kua Amesema Jabir kua: 'Sisi tulifunga Safari ambapo mmoja kati ya Wasafiri wenzetu alianguka na Kupata Jeraha la Kichwani, halafu alipolala Usiku akaota Ndoto ya Matamanio ambayo Ndani yake akajimwagia Manii.

Hivyo asubuhi yake akawauliza wasafiri wenzake kwa kusema: 'Hivi Jee mnaona Kisingizio chochote kinachoniruhusu mimi kufanya Tayammam?'

Masahaba wake wakasema: 'La Hatuoni kisingizio chochote ambacho Kitakupelekea wewe kuruhusika Kutokoga Janaba na Kufanya Tayammam badala yake.'

Hivyo Mtu huyo akachukua Maji na kukoga Janaba na baada yake akafariki. **Na tuliporudi kwa R*asul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* tukamuelezea yaliyotokea ambapo nae *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Wameshamuua mwenzao! Allah awaue na wao pia! Kwanini hawakuuliza? Hivi Jee hawajui kua Dawa ya Ujinga ni Kuuliza?.**

Kwani ilikua inatosheleza kwake yeye kufanya Tayammam na kunyunyizia matone ya Maji tu, au Kufunga Bendeji juu ya Kidonda? Na kisha akapaka Maji juu yake na Kukosha sehemu nyengine za Mwili zilizobakia.*(Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal, Sunnan Abu Daud)*

Naam tunapoiangalia Hadith ya kwanza ambayo ni ya Sayyidna Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* basi tunaona kua inasema kua Yeye alikua amevunjika Vidole vya Mkono wake wa Kulia na hivyo alifungwa Bendej na Mtabibu wa Mifupa ambae aliviunga na kuvirudisha kama vilivyokua na kisha akavishikanisha kwa Bendeji hio.

Hivyo Mbali ya kua na Hali kama hii ambapo wengi wetu leo hii ndio ingekua sababu ya Kupumzika Nyumbani lakini Sayyidna Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* aliendelea na Vita vya Jihad fii SabilI Allah huku akiwa ni Mbebaji Bendera ya Waislam, na alipouliza kuhusiana na nini afanye itakapofika wakati wa Sala kuhusiana na Udhu basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia kua apake Maji Tu Juu ya Bendej hio.

Na kwa upande wa Hadith ya pili basi tunaona ni kuhusiana na Mtu ambae alipata Ajali ya Kuanguka na hivyl akapata Jeraha la Kichwa ambalo lilikua haoitakiwi kuingia Maji. Lakini sasa katika Usiku wake Mtu huyo akajikuta ameamka na Janaba,na hivyo Kujitojarisha ni Wajibu, na kutokana na kua hajui basi akauliza kama itaruhusika kwake Kufanya Tayammam tu, lakini wenzake wakamwambia kua hana udhuru wa Tayammam wakati Maji yapo.

Na matokeo yake akakoga kwa Maji na akafariki kutokana na kuingiwa na Maji ndani ya Jeraha lake hilo la kichwani. Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akalaumu kwa kuuliza kwanini wasimwabie ajifunge bendeji tu? Kisha apake Maji juu ya Bendeji katika kukoga kwake?

Hivyo hizi ni hadith mbili zinazotumiwa na Wanazuoni kuhusiana na Udhu Bendeji na Hukmu zake ambapo kulingana nazo basi tunaona kua Wanazuoni wamezichukulia Hukmu za Hadith hizi kua inakubalika Kupaka Maji kwenye Bendeji, P.o.P, Plasta n.k pale itakapokua Mtu ana hali hiyo ya kua ni Maadhur, inapozungumziwa kuhusiana na kujitoharisha kwa Kutia Udhu, Kukoga Janaba, Hedhi, Nifasi na hata Tayamam kua kupakaza Maji Juu Yake hua ni sawa na Kupaka Maji kiungo husika.

Mbali ya kuaWanazuoni wanasema kuhusiana na Al Zubayr Ibn Khurayq kua ni Dhaif kama alivyosema Imam Ibn Hajar Al Asqallani katika Al Taqrib, lakini hata hivyo kupangusa kwenye Bendeji, P.o.P n.k kumeruhusika kutokana na umuhimu wake kulingana na dharurah gusika kama vile ambavyo inaruhusika kupangusa juu ya Soksi za Ngozi laini kutokana na vithibitihso vya hadith nyingi sana zilizosahih juu yake, jambo ambalo linapelekea kupangusa kwenye Bendeji hua nimuhimu zaidi.

Kwani anasema Imam Ibn Abd Razzaq kua: '**Amesema Imam Ibn Jurayj kua :** '**Nilimwambia Mimi Ataa kua: Kuna Mtu ambae amevunjika Mkono na hivyo Mkono wake ukafungwa Bendeji jee ni vipi kuhusiana na Udu wake?**

Ambapo Ataa akasema: '**Anatakiwa Apanguse juu yake kwa Mkono uliokua na Maji na hii itamtosheleza.'**

Lakini hua ni Lazima Kuligusa Bendeji hilo katika Kupangusa kwake, kwani Bendeji hilo hua ni sawa na Mkono wake. Hivyo Apanguse Juu yake na hata kama akikosea basi hua hamna tatizo. Kwani kuhusiana na Mkono uliokatika au Mguu basi kama ikiwa umefungwa bendeji basi tayari Mtu huyo ana sifa ya Maadhur, hivyo wacha apangusie tu Juu yake, w Allahu Aalam.'*(Musanaf Ibn Abd Razzaq)*

Na akasema Imam Al Zaylai Al Hanafi kua: '**Ama kuhusiana na Kupangusa Juu ya Bendeji au Kitu chengine kilichofunika Kidonda basi hua ni sawa na Kukosha kile Kilicho chini ya Bendeji hio.'***(Tabiyn Al Haqqaiq)*

Na akasema Imam Ibn Rushdi Al Maliki kua**: 'Kupaka Maji Juu ya Bendeji hua kunachukua sehemu ya kuikosha sehemu husika, aukuitilisha Udhu sehemu husika au Kuifanyia Tayammam sehemu husika.'***(Al Bayan wa Al Tahsil)*

Na akasema Imam Al Isnawi Al Shafii kua: **'Kupangusa Juu ya Bendeji hua ni kwenye kuchukua nafasi ya Kukosha Kiungo husika.'***(Al Muhimat)*

Na kwa upande wa Imam Al Buhuti Al Hanbal basi nae akasema kua : '**Hua ni Wajibu kupangusa juu ya Bendeji kwa sababu kupangusa juu ya bendeji hua kunachukua sehemu ya kukosha Kiungo husika.**'*(Rawda Al Murraba)*

Ambapo kwa upande wa Imam Abu Hanifa Nuuman Ibn Thabit basi yeye amesema kua: '**Ingawa Mtu asipopangusa Juu ya Bendeji hua amefanya Makosa lakini hata hivyo Udhu wake Mtu husika hua si Batili.'**

Na anasema Al Faqih Imam Ali Ibn Muhammad Ibm Habib Al Mawardi Al Shafii kua: '**Amesema Imam Al Shafii kua kama ikiwa Mtu amevunjika Kiungo cha sehemu ya mwili wake, na akafunga Bendeji na akawa hayuko Hali ya Janaba lakini akwa na Khofu kua kama Madhara yake yatazidi kama akilitoa Bendej husika basi hua kuna Mitizamo Miwili juu yake na hivyo Mtizamo uliokua Sahih baina ya Mitizamo miwili hii kutokana na Mtizamo wangu basi ni kua Sala ya Mtu husika atakayosali katika wakati huo itamtosheleza na hivyo haitokua na haja kwake kuirudia Sala hio.**

Na hali hii pia hua kwa kila kitu ambacho kinatakiwa kufanywa lakini hakiwezekani kwa Mfanyaji Ibada na kila alichoruhusiwa kukiacha katika Mambo ya Udhu.

Ambapo Mtizamo wa kwanza ni Kua atapangusa tu juu ya Bandeji lake katika Wakati wa Kutia Udhu na kisha Atasali lakini atakapopona na kuweza kutia Udhu kama kaawaida basi atarudia Sala zake hizo.

Na mtizamo wa pili ni kua haitokua na haja kwake kurudia Sala hizo, kwani kama ikiwa Hadith ya Ali ni Sahih kua alivunjika Vidole na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuamrisha Apake Maji Juu ya Bandeji yake, basi na mimi nasema hivyo hivyo.

Imam Al Mawardi Anaendelea kusema kua: Hivyo Wanazuoni Wanakubaliana akiwemo Imam Al Shafii kua Mwanammke mwenye Istihadhah hua hatakiwi kuirudia Sala na Udhu wa Sala yake hua Upo huku akiwa na Najis.

Na pia hatakiwi kuirudia Sala yule Mtu anaeumwa mbali ya kua na Maji, na pia kwa Mtu mwenye Maji lakini akawa na khofu Juu ya Kiu na hivyo akafanya Tayammam,na pia kwa Mtu asiekua na Nguo na Kusali Uchi, n.k.

Na hii ni kwa sababu ya Makubaliano yao Wanazuoni juu ya kuruhusika kwa Mfanyaji Ibada kuachana na kile asichoweza kukifanya na kuondoa Uzito wa Kuirudia Ibada husika.

Kwani Imam Al Shafii amesema kua Yeyote yule atakaekua na Maji wakati akiwa Safarini na kisha akawa anaogopa kumalizika Maji hayo na hivyo akakosa Maji ya Kunywa kuhusiana na Udhu Mtu huyo hua ni sawa na asiekua na Maji hivyo pia kwa Mtu mwenye Jeraha lenye Damu na akakhofia Matatizo zaidi kama akitia Maji basi hua ni sawa na Mtu ambae ni Tohara.

Na Imam Al Muzani amesema haya katika hali ya kua kama ikiwa Mtu alievunjika hajatia Udhu kwa khofia kifo kama atatia Udhu.

Na Imam Al Rabbi akasema haya kuhusiana na Mtu alievunjika akawa na khofu ya Kifo akitia Udhu.

Ambapo Al Muzani amemaanisha kuhusiana na Mtu ambae hakutia Udhu katika wakati wa kupangusa Bendeji na Al Rabbi amemaanisha kuhusiana na Mru ambae alitia Udhu katika wakati wa Kufunga Bendeji.

Na hivyo basi kama itakua Mtu anaepaka Maji juu ya Bendeji ameshapona basi hali yake hua haina tofauti juu ya kua kama alifunga Bendeji katika wakati akiwa na Udhu ama la.

Hivyo kulingana na Mtizamo wa Al Rabbi basi ni kua kama ikiwa Mtu alifunga Bendeji huku akiwa hana Udhu basi itambidi kurudia Sala zake baada ya kulitoa Na hivi ndivyo.pia alivyosema Al Shafii katika Al Umm, ambapo Hukmu hii ya Kupaka maji kwenye Bendeji imetokana pia na kuruhusika kupaka Maji kwenye Viatu laini vya ngozi, ambapo itambidi mtu husika pia kupaka Maji kwenye bendeji hata kama ikiwa alipolifunga alikua na Udhu.

Na hii ni kulingana na Hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* ambayo Al Shafii amesema kuhusiana nayo kua: 'Kama ikiwa Hadith hii ni sahih basi naikubali na Mtu Hatotakiwa Kuirudia Sala yake, kwa sababu amefuata Maamrisho ya Sharia na hivyo hua ni sawa na kufuta kwenye Viatu vya Ngozi laini.

Na kama Hadith hii si Sahih kutokana na Udhaifu wa Mnyororo wa Nukuu zake basi juu yake kuna Mitizamo miwili kama alivyosema Imam Al Muzani kua haina haja ya Kuirudia Sala husika kwa sababu ya Kisingizio kinachokubalika.

Na mtizamo wa pili ni wa Imam Al Rabbi ambao unasema kua Kuirudia Sala hua ni Wajibu. Kwa sababu hizi ni hali ambazo hazitokei mara kwa mara na hata kama zikitokea basi hua si za Kudumu, hivyo inaruhusika pia Kurudia Sala.''*(Al Hawi Al Kabir)*

Ama baada ya kuangalia Mtizamo wa Ima. Muhammad Idris Al Shafii, na mitizamo ya Wanafunzi wake wawili wakuu wa Misri ambao ni Imam Ismail Ibn Yahya Al Muzani Al Shafii na Imam Al Rabbi Ibn Sulayman Al Shafii kuhusiana na kuruhusika Kupaka Maji Bendeji katika wakati wa Kutia Udhu basi na tuangalie kwa upande wa Maimamu wengineo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyyah Ibn Yahya An Nawawi ambae ameegemea katika Mtizamo wa Imam Al Rabbii Ibn Sulayman Al Shafii kwa kusema:

'Hua ni Muhimu Kutia Udhu kabla ya Kufunga Bendej na hivyo kua Tohara, lakini kama ikiwa mtu hakufanikiwa kutia Udhu, basi kama itakua inawezekana kulitoa bendej basi na alitoe na kisha atie udhu, kisha ajifunge upya, lakini kama ikiwa kufanya hivyo kutasababisha Madhara Basi kufanya hivyo haitokua na haja, na hivyo kupangusa tu juu yake kutatosheleza. Hivyo kama Mtu akifunga Bendeji wakati akiwa tohara basi haitomlazimu kwake kurudia Sala zake, ambapo kwa upande mwengine basi kama Mtu akilofunga buku akiwa hana Udhu basi itambidi kurudia Sala zake akishalivua.'*(Al Majmuu Sharh Muhadhdhab)*

Naam..hii Fatwa ya Imam Al Rabbi inatukumbusha pale nilipoelezea kuhusiana na historia za Maisha ya Maimamu katika *Tabaqat Warathat Al Anabiyah* ambmo nimezungumzia pia kuhusiana na maisha ya Imam Al Muzani na Imam Al Rabii Walikua ni Ibn Ami ambao wote ni Wanafunzi wa Imam Al Shafii pamoja na Dada yake Imam Al Muzani ambae ni Mama yake Imam At Tahawi Al Hanafi.

Na tukasema kua Imam Al Rabbi alikua mbumbumbu hafahamu kitu kiasi ya kua Imam Al Shafii alikua akirudia kumsomesha Imam Al Rabbi mara 30, kuhusiana na Suali moja tu ambao wenzake kina Imam Imam Al muzani wameshalifaham baada kusomeshwa mara moja tu. Lakini matokeo yake Imam Al

Rabbi akawa anatisha kwa Ilm kiasi ya kua katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kama ikitokea kua kuhusiana na Jambo fulani wametofautiana baina ya Imam Al Muzani na Imam Al Rabbi basi Mtizamo wa Imam Al Muzani hua hauna nguvu mbele ya Mtizamo wa Imam Al Rabbii, mbali ya kua Imam Al Shafii Mwenyewe alisema kua kama kuna mtu atakaekua mrithi wake kwa Misri basi ni Al Muzani kutokana na umahiri wa Imam Al Muzani.

Hivyo Fatwa hii ya Imam An Nawawi inathibitisha hilo la kua Imam Al Rabbii alikua yuko Juu sana kwa Ilm. Na atakaetaka kujua zaidi basi na atafute kitabu Changu cha *Al Mustakshif Abu Manal Danah Tabaqat Warathat Al Anbiyah* Juzuu ya Kwanza ambacho kina Historia ya Maimamu wa Karne 2 za mwanzoni za Uislam, na kinapatikana Bure Mtandaoni.

Na tunaporudi kwa Imam An Nawawi na Udhu wa mtu mwenye Bendeji au Hogo kwa kusema kua: **‘Kuna mambo Matatu ambayo kila anaetaka kujitoharisha huku akiwa amefunga Bendeji anatakiwa ayatekeleze:**

1-Kwanza ni Lazima kukosha kwa Maji sehemu zilizokua hazikufungwa bendeji.

2-Kisha hua ni Lazima Kupangusa Bendeji nzima kwa mkono wenye Maji.

3-Kama ikiwa haiwezekani kulipaka Maji bai itambidi atumie njia ya Kutayammam.

Ambapo kwa Upande wa Imam At Tabari basi amesema kua Tayammam itatosheleza, lakini pia kuna Mtizamo usemao kua haina haja kupakaza Maji bendeji yote.’*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Ambapo kwa Upande wa Shaykh Ul Islami Imam Shams Ad Din Al Ramli Al Shafii basi yeye amesema kua: **‘Kama itakua Bendeji haiko kwenye sehemu ambayo haihitaji Tayamum basi hua haina haja ya Kurudia Sala.’***(Nihayat Al Muhtaj)*

Ambapo mtizamo huu pia umenukuliwa na Imam An Nawawi katika Rawdhat Talibin. Na kwa upande wa Al Faqih Imam Al Muhaqqiqin Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii katika Tuhfah Al Muhtaj basi yeye amegemea katika Mtizamo wa Imam An Nawawi katika Al Majmuu kama tulivyoelezea hapo kabla.

Ama kuhusiana na Tayammam basi tutazungumzia tukishamaliza mada hii ya Maadhur mwenye bendeji, hivyo viungo vya Tayammam alivyovikusudia Imam Al Ramli katika Fatwa yake basi ni Uso na Mikono.

Ama tunapoangalia kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Muhammad Alaa Ad Din Ibn Muhammad Amin Ibn Umar Abidin Al Husayni Al Hanafi ambae ni tofauti na Imam Ibn Abidin Al Shaami kua: **‘Kwa Mtu mwenye Jeraha au Bendeji na akataka Kutawadha Kusali, au kukoga Janaba na akahisi kua akitia Maji sehemu husika basi atajisababishia Madhara, basi atakapofikia katika sehemu ya Kidonda katika Kutawadha kwake au kukoga kwake basi na apanguse tu nusu ya sehemu husika.**

Na kama itakua sehemu hio ina bendeji basi na apanguse sehemu zaidi ya nusu ya sehemu husika,na kisha ataruhusika Kusali bila kutakiwa kuirudia Sala hio.’*(Al Hidaya Al Aaliyah)*

Na akasema Imam Hasan Ibn Amar Al Shurunbulali Al Hanafi kua: **'Kwa Mtu mwenye Bendeji hua inamtosheleza kupangusia Juu ya sehemu ya baina ya Mwili na Bendeji husika katika Kitawadha kwake, kukoga kwake Janaba n.k**

Na kama kuna uwezekano basi atatakiwa Kulifungua Bendeji na Kupangusa Nusu ya Jeraha kama haitomsababishia Madhara, na kama haiwezekani au itamsababishia Madhara basi apangusie Juu yake.'*(Maraqi Al Falah)*

Na akasema tena Imam Al Shurunbulali Al Hanafi kua: '**Hakuna Ulazima wa kua Mtu akifunga Bendeji lazima atie Udhu kabisa, kwani inaruhusika kwa mfano Kupangusa Juu ya Bendeji la Mguu uliojeruhiwa na kuukosha kwa kuutia Maji Mguu wa pili uliokua Mzima.**

Na wala Kupangusa huko hakutopelekea Kutenguka kwa Udhu kwa mfano kama Bendeji litatoka na hivyo inaruhusika Kufunga Bendeji jengine Jipya na kuendelea na Sala Bila kupangusa tema Bendeji hilo jipya, ila hua inaoendekezwa kupanguaa upya.'*(Nur Al Idah)*

Na akasema Al Muwaffaqa Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: **'Kama ikiwa jeraha litakua limefungwa kwa Bendeji, basi ni kama tulivyosema kua Mtu atatakiwa kukosha kukosha tu zile sehemu za Viungo zenye Afya na kwa sehemu yenye Maradhi basi atapangusa Tu. Kama alivyosema Imam Ahmad kua Kama Mtu atakhofia kua Jeraha lake litamsababishia Madhara akitia Maji, basi na apanguse pembeni yake tu na juu yake bila kutia Maji.'***(Al Mughnu)*

Na akasema Imam Muflih Al Hanbali kua**: 'Kama ikiwa sehemu ya Kiungo cha mwili kina Jeraha na hakuna khofu ya Madhara kwa kupangusia tu juu yake, basi Wanazuoni wan mitizamo miwili Juu yake.**

Ambapo Mtizamo wa kwanza ni kua Itatosheleza kupangusia Juu yake tu au kufanya Tayammam, na hivyo kupangusa huko juu ya Jeraha kutakua ni Wajibu, ambapo huu ni mtizamo sahih ulioelezewa na Shaykh Taqi Ad Din.

Na akasema pia kua kama ikiwa Mtu amejeruhiwa na akawa na khofu yakua Jeraha hilo litazidi likiingia Maji basi hua bora kupangusa tu juu ya Jeraha kuliko kupangusa juu ya bendeji, ambako nako hua ni bora kuliko Tayamam.

Na Mtizamo wa pili ni kua kwa Tu mwenye haki kama hii basi Hua ni wajibu kwake Kufanya Tayammam juu ya Jeraha ambapo huu ndio Mtizamo wa Imam Al Khiraqi, ambae amesema pia kua Wajibu hua ni Kupangusa na kutayammam.'*(Al Furuu)*

Na hapa kidogo tufahamishane pia kua ingawa Wanazuoni wamefananisha kuhusiana na Kupangusa Juu ya Bendeji na Kupangusa kwenye Soksi za Ngozi laini, Lakini hata hivyo kuna tofauti baina ya Vitu viwili hivi pale tunapoangalia kuhusiana na Mpaka wa mda wa kufanya hivyo Juu yake.

Kwani Tunapozungumzia kuhusiana na Kupngusa juu ya Khuf au Soksi za ngozi zifananazo na viatu hua na mpaka wa kua mwisho wake hua ni Siku moja kwa Mtu asiekua msafiri na kwa msafiri hua siku tatu ndio mwisho wake na wala si zaidi.

Lakini kwa upande wa Bendeji au Hogo au Plaster n.k basi mwisho wake hua hadi pale Mtu atakapona na kuhitajika kuitoa.

Na pili kwa upande wa Soksi basi hua inatakiwa Mtu husika awe na Udhu katika wakati kuvaa kwake nankisha ndio ataruhusika kupangusia maji juu yake, lakini kwa upande wa Bendeji au Hogo au plaster hua hakuna ulazima wa kua na udhu kwa sababu Bendeji huvaliwa kutokana na Majeraha na hua Mtu hua hawezi kujijeruhi kwa khiari yake, hivyo hua hakuna ulazima wa Kutia udhu kabla ya kufunga Bendeji ili baadae uje kupangusia Maji tu katika wakati wa Kutia Udhu.

Ama baada ya kuangalia Mtizamo ya Wanazuoni wa Madhhab tofauti kuhusiana na Kuruhusika Kupangusa Bendeji, P.o.P, Plaster n.k basi na tumalizie kuhusiana na Mada hii kwa mambo hitimisho linalojumuisha mambo yafuatayo:

1-Hairuhusiki Kwa Mtu alievaa Bendeji Mguuni, Kisha akavaa Khuf yaani Viatu vya Ngozi laini kupangusa Mguu Kwa Juu ya Viatu hivyo katika wakati wa kutia Udhu na hii ni kama alivyosema Imam Al Shirbini kua: '**Kama ikiwa Mtu atavaa Khuf Juu ya Bendeji, basi hatoruhusika Kupangusa juu ya Bendeji katika wakati wa kutia Udhu na hii ni kwa sababu kupangusa huko hua ni kupangusa kwenye ya kitu ambacho imeruhusika kupangusa Juu yake kama vile ambavyo inapokua Mtu ana bendeji ya Kichwa kisha akavaa na Kilemba na kupangusa Juu ya Kilemba.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Na imesemwa katika Mawsuah Ahkami Al Wudhuu kua: '**Miongoni mwa Masharti ya kuruhusika kupangusa juu ya Bendeji ni kutodhuru Kiungo kilichojeruhiwa,au Kidonda husika, na kua na khofu ya Kudhurika kiungo husika kutokana na kuondolewa kwa Bendeji.**

Hivyo kama ikiwa Kupitisha Maji kwenye kiungo husika hakutosababisha madhara, na hakuna madhara ya kuondoa Bendeji basi hapa kukosha kwa maji kiungo husika hua ni Wajibu. Kwa Sababu Kukosha kwa Maji Kumeruhusika kutotekelezwa kwake kutokana na Dharura, hivyo kama ikiaa hakuna Dharurah basi kukosha hua inabidi kutekelezwa, na hakuna kutokukubaliana kwa Wanazuoni juu ya Hili.'*(Mawsuah Ahkami Fiqhiyyah)*

Ama kuhusiana na Idadi ya kupangusa basi Wanazuoni wa Madhhab yote wanakubaliana kua Ingawa kila kiungo hua ni Sunna kukosha mara tatu katika wakati wa Kutia Udhu lakini kwa upande wa Kupangusa Bendeji, au Hogo au Plasta n.k hua kunatakiwa iwe ni mara Moja tu.

Na Wanazuoni wa Madhhab yote Wanakubaliana kua; Ili Mtu aruhusike kupangusa Bendeji, P.o.P, Plasta n.k basi Bendeji Husika liwe Limetumika kwa Makusudio yake stahiki, yaani isiwe kama vile mtu avelifunga au amelivaa kwa ajili ya kuukaza Msuli fulani, bali iwe kwa ajili ya kiungo kilichovunjika, Jeraha au Kidonda Na hivyo Kufunguliwa kwake itasababisha kuchelewa kupona kwa Kidonda, Kuchelewa Kuunga kwa Mfupa,n.k.

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA UDHU KWA KUGUSA SEHEMU ZA SIRI

❖❖❖❖

Naam..tuko katika kukumbushana kuhusiana na Aina za Sujud katika Uislam na Utekelezwaji wake. Ambapo ndani ya aina hizo za Sijda basi tunakutaka na Sijda Muhimu kuliko zote zinazowatofautisha Waumini wa Dini ya Kiislam na wa Dini nyenginezo Duniani ambayo ni Sijda ya Ndani ya Sala ya Kiislam ambayo ndio Msingi wa Ibada ya Sala unaodhirisha Unyenyekevu Kiumbe kwa Muumba.

Na Alhamd lillah tumeshaangalia mengi sana kwani tumeanza mwanzo wa Ibada ya Sala hatua kwa hatua, masharti yake, Nguzo zake na Sunnah zae kulingana na Mitozamo ya Wanazuoni wa Madhhab tofauti hadi kufikia kwenye yale yanayobatilisha Sala, kwa kuanzia kwenye yabatilishayo Udhu kwani bila ya Udhu basi hua hakuna Sala, na kwa kua Udhu hua unaenda Sambamba na Tayammam basi tumeangalia kuhusiana na Tayammam pia.

Na kwa kua yanayobatilisha Udhu basi Hua yanabatilisha na Tayammam pia na hivyo kubatilisha Ibada ya Sala na Sujud zilizofanywa ndani yake basi na tuendelee kukumbushana yanayobatilisha Udhu ambayo hatujayaangalia bado.

Hivyo umefikia wakati wa kukumbushana kuhusiana na Kutenguka au kubatilika kwa Udhu na Sala kutokanako na Mtu kujigusa sehemu za Siri Kwani anasema Imam Abu Abd Rahman Ahmad Ibn Shuayb Ibn Ali Ibn Sinan Ibn Bahr Ibn Dinar Al Khurashi An Nasai Al Shafii kua:

أَخْبَرَنَا هَارُونُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، حَدَّثَنَا مَعْنٌ، أَنْبَأَنَا مَالِكٌ، ح وَالْحَارِثُ بْنُ مِسْكِينٍ قِرَاءَةً عَلَيْهِ وَأَنَا أَسْمَعُ، عَنِ ابْنِ الْقَاسِمِ، قَالَ أَنْبَأَنَا مَالِكٌ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ أَبِي بَكْرِ بْنِ مُحَمَّدِ بْنِ عَمْرِو بْنِ حَزْمٍ، أَنَّهُ سَمِعَ عُرْوَةَ بْنَ الزُّبَيْرِ، يَقُولُ دَخَلْتُ عَلَى مَرْوَانَ بْنِ الْحَكَمِ فَذَكَرْنَا مَا يَكُونُ مِنْهُ الْوُضُوءُ فَقَالَ مَرْوَانُ مِنْ مَسِّ الذَّكَرِ الْوُضُوءُ . فَقَالَ عُرْوَةُ مَا عَلِمْتُ ذَلِكَ . فَقَالَ مَرْوَانُ أَخْبَرَتْنِي بُسْرَةُ بِنْتُ صَفْوَانَ أَنَّهَا سَمِعَتْ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ يَقُولُ " إِذَا مَسَّ أَحَدُكُمْ ذَكَرَهُ فَلْيَتَوَضَّأْ

‘**Amesema Harun Ibn Abd Allahi kua ametuambia Maa’n kua Malik ametuambia sisi na Harith Ibn Miskiina alikua akimsomea na mimi nilikua namsikiliza akisema kua amesema Ibn Al Qasim kua amesema Malik kua amesema Abdillahi Ibn Abi Bakr Ibn Muhammad Ibn Amir Ibn Hazim Kua amemsikia Urwa Ibn Zubayr kua Nilienda mimi kwa Marwan Ibn Al Hakam na tukazunvumzia Vitu vinavyobatilisha Udhu. Ambapo Marwan akasema kua Udhu unatakiwa Utiwe tena baada ya Mtu Kujigusa Dhakar.**

Urwa akasema: Mimi sijui juu ya hilo Marwan akasema: Ameniambia mimi Bushra Bint Safwa *Radhi Allahu Anha* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Na kama ikiwa yeyote yule Mmoja wenu kati yenu atajigusa Dhakar yake basi itambidi atie Udhu.’ *(Sunan An Nasai)*

Hivyo hii ni moja kati ya Hadith zinazosisitiza umuhimu wa Kutia Udhu baada ya mtu kujigusa sehemu zake za Siri iwe Mtu huyo ni Mwanamme au ni Mwanammke.

Mbali ya kua kuna hadith pia isemayo kua**:**

وَعَنْ طَلْقِ بْنِ عَلِيٍّ – رضى الله عنه – قَالَ: { قَالَ رَجُلٌ: مَسَسْتُ ذَكَرِي أَوْ قَالَ اَلرَّجُلُ يَمَسُّ ذَكَرَهُ فِي اَلصَّلَاةِ, أَعَلَيْهِ وُضُوءٌ ? فَقَالَ اَلنَّبِيُّ – صلى الله عليه وسلم –"لَا, إِنَّمَا هُوَ بَضْعَةٌ مِنْكَ } أَخْرَجَهُ اَلْخَمْسَةُ, وَصَحَّحَهُ اِبْنُ حِبَّانَ

Amesema Talq Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu* kua: Kuna Mtu alisema "Nimejigusa Dhakar yangu", au alisema "Hivi Jee kama Mtu akijigusa Dhakar yake Katika wakati wa Sala anatakiwa Atie Udhu?'

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'La Haina haja kwa sababu hio ni sehemu ya Mwili wako.' *(Sahih Ibn Hibban, Bulugh Al Marami, Sunnan Abu Daud, Sunnan An Nasai, Sunnan At Tirmidhii, Sunnan Ibn Majah na Musnad Imam Ahmad Ibn Hanbal)*

Ambapo ingawa hii ni Hadith yenye Sifa ya kua ni Hasan Hadith kulingana na Vigezo vya Maimamu walioinukuu. Lakini hata hivyo kwa upande wa Imam Ibn Hazim Al Andalus amesema kuhusiana na Hadith hii kua: **'Hadith hii ya Talq Ni hadith Sahih isipokua ni hadith isiyokua na Uthibitisho ndani yake. Na hii ni kwa sababu kwanza Hadith hii inakubaliana na yale ambayo waliyokua wakiruhusika kuyafanya watu kabla ya kuja kwa amrisho la Kutia Udhu baada ya kujigusa Sehemu za Siri, na hakuna shaka juu ya hili.**

Na hivyo basi Hukumu yake hadith hii imebatilishwa pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoamrisha Kutia Udhu baada ya Kujigusa sehemu za Siri. Na hua hairuhusiki kwa Mtu kuacha kile ambacho mtu ana uhakika kua ni batilisho na kuchukua kile ambacho ana uhakika kua kimebatilishwa.

Sababu ya pili ni kua maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yasemayo kua : Kwani hio ni sehemu ya Mwili wako. Ambayo yanadhihirisha kua hii ilikua ni kabla ya amrisho la Kutia Udhu baada kujigusa sehemu za Siri, kwa sababu kama ingekua ni baada yake basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salaam* asingesema maneno haya, bali angeweka wazi kua Hilo ndio amrisho' *(Al Muhalla)*

Baada ya kuangalia Hadith mbili ambazo ni zenye kupingana kuhusiana na Kujigusa sehemu za Siri baada ya Kutia Udhu ambapo Moja wapo imesema kua Udhu unabatilika na ya pili inasema kua haubatiliki. Lakini hapo hapo tumeona pia Wanasema kua Hadith ya kwanza ya kua Udhu unabatilika imeinatilisha Hadith ya pili na kwa maana hio basi Udhu hua Unabatilika.

Hivyo mbali ya kuangalia hadith mbili hizo basi kabla ya kuzama kwenye Mitizamo ya Wanazuoni wa Skuli za Madhhab ya Fiqh ili kupata Fatwa tofauti juu ya jambo hili ili tupate kujua tunasimamia wapi, na bila ya shaka hatuwezi kujua bila kuangalia Mitizamo ya Wanazuoni wa Fiqh kulingana na Madhhab yao na hapa ndio tunaona kua Muislam haiwezekani kuchukua Hadith na kuifanyia kazi bila kujua tukio lililompelekea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusema Maneno ya Hadith husika,kwani hapo ndio utajua asili ya Hadith, wakati wake, imebatilishwa na Hadith nyengine au na Aya ama la, usahih wake, udhaifu wake n.k. Na bila ya shaka kama hujui haya basi Utapotoka tu.
Hivyo ili tusipotoke basi inabidi tufuate maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema:

﴿ فَسْـَٔلُوٓاْ أَهْلَ ٱلذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ﴾

Fas-al Ahl Al Dhikr in kuntum la Taalamun - Waulizeni wanaojua kama ikiwa nyinyi hamjui*(Surat An Nahl 16:43)*

Na Ahl Al Dhikr ni Maimamu wa Madhahab. Ambapo kabla ya kuwauliza Wanazuoni wa Fiqh basi na tuangalie hadith nyengine ambazo zinasema kua:

قال الدارقطني في السنن: ثنا محمد بن مخلد، ثنا حمزة بن العباس المروزي، ثنا الحسين بن إسماعيل، ثنا يحيى بن مُعلى، نا عتيق بن يعقوب، حدثني عبد الرحمن بن عبد الله بن عمر بن حفص العمري، عن هشام بن عروة، عن أبيه، عن عائشة أن رسول الله –صلى الله عليه وسلم– قال: ويل للذين يمسون فروجهم ثم يصلون ولا يتوضئون، قالت عائشة: بأبي أنت وأمي هذا للرجال، أفرأيت النساء؟ قال: إذا مست إحداكن فرجها فلتتوضأ للصلاة ثم قال: عبد الرحمن العمري ضعيف.

Amesema Ad Daraqutni kua Muhammad Ibn Mukhallad kua amesema Hamza Ibn Abbas Al Marwazi kua amesema Al Husayn Ibn Ismail kua amesema Yahya Ibn Mualla kua amesema Atiq Ibn Yaqub kua amesema Abd Rahman Ibn Abd Allah Ibn Umar Ibn Hafs Al Umari kua amesema Hisham Ibn Hisham Ibn Urwa kua amesema Baba yake kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ole wao wale ambao watajigusa sehemu zao za Siri na kisha Wakasali bila ya kutia Udhu.'

Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema: 'Baba yangu na Mama yangu watolewe kafara kwa ajili yako ya Rasul Allah, hivi usemavyo ni kwa ajili ya Wanaume, ila Jee ni vipi kuhusiana na Wanawake?'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Yeyote yule Miongoni mwenu (Wanawake) atakaejigusa sehemu za Siri basin a akatie Udhu.'(Sunnan Ad Daraqurni)*

Naam..tumeiangalia hadith hii kwa makusudi kwa sababu ni Hadith yenye kuwazungumzia Wanawake pia jambo ambalo ni tofauti na zile hadith za awali zinazowazungumzia Wanaume tu. Na tunapoiangalia hadith hii ambayo tutaifafanua tena baadae Inshaa Allah basi tunaona kua Imam Ad Daraqutni anasema baada ya kumalizia Hadith hii kua: '**Abd Rahman Al Umari ni Dhaifu wa Hadith.'**

Lakini hapo hapo kuna Hadith nyengine ya Aisha *Radhi Allahu Anha* kutoka kwa Imam An Nasai isemayo kua:

وقال الحراني: أنبأتنا عفيفة، قالوا: أنبأ فاطمة الجوزدانية، أنا ابن ريذة، أنا أبو القاسم سليمان بن أحمد بن أيوب اللخمي، أنا أحمد بن عبد الله بن العباس الطائي البغدادي، ثنا أحمد بن سعيد الهمداني، ثنا أصبغ بن الفرج، ثنا عبد الرحمن بن القاسم، عن نافع بن أبي نعيم ويزيد بن عبد الملك النوفلي، عن سعيد المقبري، عن أبي هريرة قال رسول الله –صلى الله عليه وسلم–: إذا أفضى أحدكم بيده إلى فرجه ليس دونها حجاب فقد وجب عليه الوضوء

Amesema Al Harun kua ametuambia sisi Afifi kua amesema Amesema Fatma Jawzdaniyat kua amesema Abd Ridat kua amesema Abu Al Qasim Ibn Sulayman Ibn Ahmad Ibn Ayub Al Khamiy kua amesema Ahmad Ibn Abd Allahi Ibn Al Abbas Al Tai Al Baghdadi kua amesema Ahmad Ibn Said Al Hamdani kua amesema Asbagh Ibn Al Faraj kua amesema Abd Rahman Ibn Qasim kua amaesema Nafi Ibn Aji Naim na Yazid Ibn Abd Al Malik Al Nawfal kua amesema Said Al

Maqburi kua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kama ikiwa Mmoja wenu ataweka Mkono wake kwenye Sehemu zake za Siri Bila ya Kua na Kizuizi baina ya Mkono wake na Sehemu zake za Siri basi Udhu humuwajibikia Mtu huyo.'*(Mustadrak Al Hakim, Tahmid ya Imam Ibn Abd Al Barr)***

Na anasema Imam Ibn Abd Al Barr: '**Ama kuhusiana na Mitizamo ya Miongoni mwa Masahaba *wa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wanaounga Mkono kua Kila atakaejigusa sehemu za Siri wakati akiwa na Udhu basi Udhu hua ni Wajibu kwake ni pamoja na Umar Ibn al Khattab, Abd Allah Ibn Umar, Abu Hurayrah, Al Bara Ibn Azib, Zayd Ibn Khalid Al Juhani, Jabir Ibn Abd Allah na Saad Ibn Abi Waqas *Radhi Allahu Anhum.***

Ama kuhusiana na Maimamu wa Tabiina yaani kizazi kilichofuatia baada ya Masahaba *Radhi Allahu Anhum* basi wenye Mtizamo huu pia ni pamoja na Imam Said Ibn Musayyib, Imam Ataa Ibn Abi Rabah, Imam Tawus, Imam Urwa, Imam Sulayman Ibn Yasir, Imam Aban Ibn Uthman, Imam Ibn Shihab, Imam Mujahid Ibn Sulayman, Imam Makhul, Imam Jabir Ibn Zayd, Imam Hasan Al Basr na Imam Ikrimah na hii ni kulingana na kama ilivyoelezewa katika Musanaf Ibn Abi Shaybah na Musanannaf Ibn Abd Razzaq.

Ama kwa upande wa Maimamu waliofuatia baada kizazi cha Tabiina yaani cha Tabji Tabiina wenye Mtizamo huu ni pamoja na Imam Muhammad Idris Al Shafii, Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Al Awzai, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Ahmad Ibn Hanbal Imam Daud na Imam At Tabari.' *(Imam Ibn 'Abd al-Barr katika Al-Tamhīd)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Shafii na Imam Ibn Hanbal basi mbali ya kua wanakubaliana juu ya hili lakini hata hivyo kila mmoja ametumia Ufafanuzi wake na hivyo kuna kutofautiana kulingana na Hadith walizotumia kila mmoja wao juu ya mada hii. Na kwa upande wa Imam Malik nae ingawa anakubaliana na Mtizamo huu pia lakini ufafanuzi wake ni tofauti pia kama tutatakavyoona.

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua Kujigusa Mtu sehemu za Siri iwe mtu huyo ni mwanamme au Mwanammke iwe sehemu za Siri za Mbele au za Nyuma basi hua hakubatilishi Udhu wala Sala. Ambapo hapa pia itabidi tutoe ufafanuzi wao na vithibitisho vyao.

Ambapo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambao wanasema kua: **'Kujigusa sehemu za Siri iwe za mbele au za Nyuma kwa Mwanamme au kwa Mwanamke hua hakubatilishi Udhu.'** *(Maraqi Al Falah)*

Anasema Al Khatib Al Aallmah Imam Shams Ad Din Muhammad Jbn Muhammad Ash Shirbini Al Shafii kua: '**Kuna Makubaliano ya Wanazuoni katika Madhhab ya Imam Al Shafii kua Kugusa sehemu za Siri kwa Matumbo ya Viganja vya Mikono hua kunatengua Udhu. Na tunapozungumzia kuhusiana na Sehemu za Siri za Mwanamme zinazotengua Udhu basi ni Dhakar yake tu lakini Korodani zake hua hakutengui Udhu.**

Na kwa Upande wa Mwanammke basi Udhu utatenguka Kama atagusa Mashavu Madogo ya Ndani ya Uke lakini akigusa Mashavu ya Nje basi Udhu haubatiliki, na pia akigusa Maziwa yake hua haubatiliki. Ama kuhusiana na Sehemu za Siri za Nyuma basi kama Mtu akigusa Tundu ya Haja Kubwa Udhu utakua Umemtoka iwe Mtu huyo ni Mwanamme au Mwanammke.

Na kuhusiana na Sehemu za Siri hizi zinazotengua Udhu basi hua zinajumuisha za Ibn Adam wote iwe mtu amejigusa yeye mwenyewe au amemgusa Mwenzake.'*(Al Mughni Al Muhtaj)*

Na amesema Imam Shuhab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Naqib Al Misri Al Shafii katika Umdat Salik wa Uddat An Nasik kua: '**Udhu wa Mtu hua unabatilika kwa Kugusa sehemu za Siri za Mbele au Tundu ya Haja Kubwa kwa kutumia Sehemu za Ndani za Viganja vya Mikono au za Vidole.**

Bila Kuzingatia kama Kugusa huko kwa Mtu husika kunatokana na Bahati mbaya, kwa Makusudi, kwa Matamanio ama la, kugusa sehemu za Siri za Mbele ama za Nyuma,Kujigusa Mwenyewe au kumgusa Mtu mwengine, iwe Mtu alieguswa ni Mwanamme au Mwanammke, Iwe amekufa au yuhai.

Ila Udhu hautobatilika kama Mtu akijigusa kwa kutumia Ncha za Vidole, kwa kutumia Sehemu za Pembeni baina ya Vidole Nyuma ya Mkono.'*(Umdat Salik)*

Na akasema Mujaddid Ad Din Imam Al Madhhab Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Kama Mtu akijigusa Korodani zake, Makalio yake au Magoti yake bila Kugusa Uume wake basi Udhu hautenguki.**'*(Al Umm)*

Na imesemwa katika Mawsuah Al Ahkami Fiqhiyyah kua: **'Kugusa Korodani Mbili, Mashavu Mawili ya Nje ya Uke na Makalio hua hakutengui Udhu,na juu ya hili kuna makubaliano ya Wanazuoni wa Madhhab ya Hanafi, Maliki, Shafii na Hanbali na hivo ndivyo wasemavyo wengi Miongoni wa Wanazuoni kwa sababu hakuna Uthibitisho uoneshao kua Kugusa Korodani, Makalio, au Mashavu yasiyokua ya Ndani ya Uke kua Kunabatilisha Udhu, hivyo Kanuni zinasema kua Udhu hua unakuwepo. Na hua haiwezekani kuhukumu kua Unabatilika wakati hakuna Uthibitisho.'**(*Mawsuat Ahkami Fiqhiyyah)*

Na akasema Shayhk Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: **'Wanazuoni wetu Wanasema kua: Kugusa Korodani, na Nywele za Sehemu za Siri za Mwanamme na Mwanammke hakubatilishi Udhu, wala kugusa sehemu ya baina ya Tundu ya Haja ndogo na Tundu ya Haja kubwa, wala eneo la Baina ya Makalio. Bali kunakobatilisha Udhu hua ni kugusa Dhakari, Sehemu ya Makutano ya Mashavu ya Ndani na ya Nje ya Uke na Tundu ya Haja kubwa, na hivyo Mwanamke kama akigusa Nje ya Mashavu makubwa basi Udhu haujatenguka.'***(Al Majmuu)*

Anasema Shaykh Ul Islami Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Zayn Ad Din Al Sunayki Al Ansari Al Shafii kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Kama mtu akijigusa sehemu za Siri kwa mikono yake bila ya kuwpeo kwa kizuizi baina yake basi na atie Udhu.'(***Imam At Tirmidhii, Imam Ibn Hibban)*

Ambapo kumgusa Mtu mwengine hua ni vibaya zaidi kwani hua ni kumvunjia Heshima Mtu husika jambo ambalo ni haki yake mhusika.'*(Asna Matalib Sharh Rawdat Talib)*

Kisha Imam Zakarriyah Al Ansari anaendelea kutuambia kua: **Kugusa kwa Kiganja cha Mkono kumewekwa ndani ya Mipaka ya Kugusa kutokana na Hadith husika**. **Na hivyo humaanisha kutumia sehemu za Ndani ya Viganja (Tumbo la Kiganja) hata kwa kugandamiza japo kidogo, na hivyo hii haimaanishi kwa kutumia Ncha za Vidole au Kutumia sehemu zilizo baina ya Vidole au Upande wa Nyuma wa Kiganja hivyo kugusa kwa kutumia sehemu hizi hua hakubatilishi Udhu Kwa sababu sehemu za Ndani ya Kiganja *(Batin Al Kaff)* ni Sehemu zenye kuamsha Hisia zaidi za Matamanio katika kugusa, tofauti na kugusa kwa sehemu ya kiungo chengine au kwa kitu chengine.'** *(Asna Matalib Sharh Rawda Talib)*

Imam Zakarriyah Al Ansari anaendelea kusema kua: '**Ama kuhusiana na alieguswa basi hua Udhu wake haubatiliki, tofauti na Mgusaji na hii ni kwa sababu Hukmu inamhusu anaegusa na wala si anaeguswa.'***(Asna Matalib fi Rawdha Talib)*

Ambapo kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibm Sharaf An Nawawi Al Shafii basi anaelezea zaidi kuhusiana na Matumbo ya viganja kubatilisha Udhu kupitia katika hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema: '***Idha Ifdha Ahadakumu biyadihi ila Farjahu Laysa Duniha Hijaban Faqad Wajiba Aalayhi Al Wudhuu-*** **Kama Ikiwa Mmoja wenuataweka Mkono wake kwenye Sehemu za Siri bila Kizuizi baina yake basi Humuwajibikia Udhu. Neno *Ifdha* hua linatumika kumaanisha kitu kinachofanywa na Kiganja cha Mkono, kwani vyenginevyo hua linamaanisha Kuingiliana kimwili, na Al Shafi amesema katika Al Umm kua Ifdha hua kinatumika kwa kutumia Viganja vya Mikono kama vile mtu asemavyo Ameweka Mikono yake ardhini katika Kusujudu au ameweka Mikono yake Magotini katika Kurukuu, au ameweka Mikono yake yake viganja vyake, ambapo haya ni maneno ya Al Shafii katika Al Umm Kwa Sababu sehemu ya Nyuma ya Viganja hua si Viungo vya Kugusia yaani raha huweza kupatikana kutokana na kugusa kwa Matumbo ya Viganja.'***(Al Majmuu)***

Naam,baada ya kuangalia mitizamo ya Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Kutenguka kwa Udhu kwa mtu alieguaa sehemu za Siri basi na tumuangalie Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Al Hafidh Imam Shihab Ad Din Abu Fadhil Ahmad Ibn Nur Ad Din Ibn Ali Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani ambae anafafanua kuhusiana na vitihibitisho ya Madhhab ya Imam Al Shafii katika kitabu chake cha Talkhis Al Kabir kwa kutuambia kua:

'**Ama kuhusiana na hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua Yeyote yule atakaweka Mkono wake kwenye sehemu zake za Siri bila ya kuwepo Kitu baina yake basi Udhu humuwajibikia iliyonukuliwa na Ibn Hibban katika Sahih yake kutoka kwa Nafii Ibn Nuaym na Yazid Ibn Abd Al Malik ambao wote wamenukuu kutoka kwa Said Ibn Maqburi kutokea kwa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* basi sisi (Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii) tunasema kua: 'Uthibitisho wetu kutokana na Hadith hii ni kutoka kwa Nafi' na wala si kutoka kwa Yazid Ibn Abd Al Malik.''**

Hivyo hii ni Hadith sahih na Mnyororo wake wa Nukuu ni wenye kuaminika sana na Al Hakim amesema kua ni Hadith Sahih. Na Ibn Sakn amesema kua Hii ndio Hadith bora zaidi kuhusiana na Mada hii. Na Ibn Abd Al Barr amesema kua Hadith hii ilikua haijulikani isipokua kupitia kwa Yazid hadi pale Imam Al Asbagh alipoinukuu kutoka kwa Ibn Al Qasim Kupitia kwa Nafi'i Ibn Nuaym na Yazid ambao wote wameinukuu kutokea kwa Al Maqburi, hivyo hii ni Hadith Sahih kabisa.

Isipokua Ahmad Ibn Hanbal hakuridhika na Nafii Ibn Abi Nuaym katika Hadith bali ameridhika nae katika Kiraa cha Qur'an, ambapo Imam Yahya Ibn Main hakukunaliana na Ahmad Ibn Hanba na hivyo akaisahihisha Hadth hii.'*(Talkhis Al Kabir Fii Takhrij Al HadithAl Rafii Al Kabir)*

Hivyo Wanazuoni wetu wameitumia Hadith hii kama uthibitisho wa kua kubatilika kwa Udhu hutokea pale itakapokua Tumbo la Kiganja cha Mkono kimeshika sehemu za Siri kama lilivyosema neno Ifdha, kwa sababu sharti linaonesha kua Mkono wenyewe haubatilishi Udhu isipokua Tumbo la Kiganja cha Mkono ndio libatilishalo Udhu.'*(Talkhis Al Kabir Fii Takhrij Al HadithAl Rafii Al Kabir)*

Ambapo katika Ufafanuzi wake Imam Ibn Hajar Al Asqallani amesema kua Imam Ahmad Ibn Hanbal hakuridhika na Imam Nafii katika Ilm ya Hadith bali anamkubali katika Ilm ya Kisomo cha Qur'an kwa sababu Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na Suali hili kidogo uko tofauti kwani Imam Ahmad Ibn Hanbal na Imam Al Awzai wao wanasema kua: '**Hakuna tofauti juu ya kubatilika kwa Udhu kutokana kugusa Sehemu za Siri kwa Tumbo la Kiganja cha Mkono au Kwa Mgongo wa kiganja cha mkono.'**

Kama anavyosema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali katika Al Mughni kua: '**Hakuna tofauti ya Kihukmu kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu kwa kugusa kwa Tumbo la Kiganja cha Mkono au Nyuma ya Kiganja cha Mkono, ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Ataa na Al Awzai Lakini mwa upande wa Imam Malik na Imam Al Shafii na Imam Is-haq Ibn Rahawayh basi wao wanasema kua: Udhu haubatiliki isipokua pale Tumbo la Kiganja litakapogusa sehemu za Siri.'***(Al Mughni)***

Ambapo kwa upande wa Imam Ali Al Mawardi Al Shafii anasema kua: **'Imam Abu Ali Ibn Abu Hurayrah amenukuu kutoka kwa Mujaddid Ad Din Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Idris Al Shafii kwa kusema kua: Kugusa hua kunajulikana kwa kua na hali sawa kimazingira baina ya kutumia Tumbo la Kiganja na Mgongo wa Kiganja, Ila kihisia basi Nyuma ya Kiganja cha Mkono hua hakubatilishi Udhu kwa sababu ya Kukosekana kwa Hisia katika upande huo wa Mkono**.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Na amesema Imam Al Khattabi kua: '**Kugusa sehemu za Siri za Mwanamme kwa kutumia mkono wa Kulia kunakirihisha na hii ni kutokana na kutakiwa kuuzuia Mkono wa kulia kugusa sehemu ambazo huenda zikawa si tohara*, kwani Rasul Allah Salallahuu Alayhi wa Salam* alikua akiutumia mkono wake wa kulia kwa ajili ya Kula, Kunywa, Kuvaa nguo, a kuutumia mkono wake wa Kushoto kwa ajili ya mambo mengine.'**

Baada ya kuangalia mitizamo ya Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu baada ya Kugusa sehemu za Siri basi na tumkamate Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Abi Al Alaa Idris Ibn Abd Rahman Ibn Abd Allah Ibn Yalin Ibn Sanhaj Al Said Al Bahfashimi Al Bushi Al Bahnasi Al Masri Al Qarafi Al Maliki ambae ni Mwanafiqh wa Madhhab ya Imam Malik maarufu. Kwa Jina la Imam Al Qarafi Al Maliki. Hivyo Imam Al Qarafi Al Maliki anatufafanulia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik kuhusiana na Hukumu ya Kugusa Sehemu za Siri wakati mtu akiwa na Udhu kwa kusema kua:

'Kuna tofauti baina ya Kugusa sehemu za Siri kwa Tumbo la Kiganja kulingana na Mtizamo wa Imam Malik kama ilivyosema Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Allahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule mmoja wenu atakaegusa sehemu zake za Siiri basi na atie Udhu. Ufanyaji kazi lakini pia Vidole hua havina hisia zaidi kuliko Tumbo la Kiganja na hivyo haviwezi kujumuishwa ndami ya Hukmu hii, kama alivyosema Imam Ash Shabi.

Ambapo Watu wa Morocco na baadhi ya watu wa Baghdad hua hawaelezei hisia za Raha kutokana na Hisia za Vidole, lakini kwa upande wa Watu wa Iraq hua wanaelezea Hisia za Raha kutokana na Vidole kwa kulinganisha na hisia zipatikanazo pale wanapowapapasa Wanawake.

Na kutokana na Hadith ya Talq *Radhi Allahu Anhu* pale *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoulizwa kwa kusema: 'Ya Rasul Allah! Hivi Jee unafikiriaje kuhusiana na Mtu aliejigusa sehemu za Siri baada ya Kutia Udhu?''

Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibu kwa kusema kua: 'Hivi Jee Hio si sehemu ya Viungo vyako Mwili? Hivyo Watu wa Iraq wamesema kua Hadith kuhusiana kua na Hisia na kutokua na Hisia zitakiwa kupatanishwa.'

Hapa nataka tufahamiane kidogo kua katika Kuelezea kwake Imam Al Qarafi basi anapowazungumzia watu wa Iraq hua anamaanisha watu wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Watu wa Maghribi au Morocco kama Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik. Kwani huo ndio uhalisi ulivyokua katika wakati huo na hadi leo kabla kuja Uwahabi, Uansari au Usalafi n.k kua Ikisemwa waislam wa Afrika Mashariki basi hua inamaanishwa wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Na kuhusiana na kuzipatanisha baina ya Hadih mbili hizo basi ni kama alivyosema Imam Al Sanani kua: **'Mtizamo unaopendelewa na kukubalika zaidi ni juu ya Ubatilisho, na kutokan ana kua Hadith ya Bushra ni yenye nguvu zaidi, kutokana na wingi wa Wanazuoni ambao wameipitia na kusema kua sahihi na kutokana na kua na vithibitisho vingi zaidi, vile vile tunapoiangalia Hadith ya Bushra basi tunaona kua alinukuu wakati akiwa na Muhajjirin na Ansari, sehemu ambayo kulikua na watu wengi ambapo hakuna hata mmoja aliepinga juu yake hadithi hio**.*(Subulan Salam)'*

Na hii ni kwa sababu Hadith ya Bushra Bint Safwa *Radhi Allahu Anha* basi ni sahih zaidi kwa kuliko Hadith ya Talq Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu* ambayo Wanazuoni wengi wamesema kua ni dhaif miongni mwao akiwemi Imam Al Shafii, Imam Abu Hatim, Imam Abu Zurag, Imam Al Bayhqi, Imam Ad Daraqutni na Imam Ibn Al Jawzi, wakati Imam Al Bukhari amesemkuhusian na hadith ya Bushra Bint Safwa *Radhi Allahu Anha* kua: '**Ndio Hadith sahih Zaidi kuliko zote katika hadithi zenye kuzungumzia mada hii.'**

Na pia sababu Hadith ya Bushra Bint Safwa *Radhi Allahu Anha* n hadith ambayo imenukuliwa na Masahaba Kumi na Saba *Radhi Allahu Anhum,* wakati Hadith ya Talq Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu* haina wathibitishaji waliokua wengi, hivyo Haidith ya sababu Hadith ya Bushra Bint Safwa *Radhi Allahu Anha* ni Hadith inayokubalika kutokana na kua na sifa yenye salama zadi kufuatwa.

Ambapo Imam Al Qarafi anaendelea kusema kua **: 'Kulingana na Mtizamo wa watu wa Iraqi au Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi Udhu haubatiliki kwa kugusa sehemu za Siri. Lakini kulingana na Mtizamo wa watu wa Morocco au Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: Kiganja na Vidole vimeainishwa kiumaalum kiwajibu na hivyo hadith hizi mbili haina haja ya Kuzipatanisha kwa sababu Hadith ya Talq ni hadith ambayo imebatilishwa Lakini wafuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wametoa Hoja 10 kuhusiana na Hadith ya Bushra ambapo miongoni mwao ni kutokubalika kwa Hukmu hio na Wanazuoni Masahaba akiwemo Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu anhu* ambae alipoambia kuhusiana nayo basi akasema kua: 'Sijali Mimi kama ikiwa nimegusa sehemu za Siri au kama Nimegusa ncha ya Pua Yangu. Na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* amesema kua Kama Unaona kua Kuna kitu si Tohara kwenye Mwili wako basi kikate'**

Ambapo Imam Al Qaraf Anasema kua: '**Hoja hizo zimejibiwa kua: Kama Hadith itakua si sahih kwa Mmoja basi kwa Mwengine inaweza kua ni Sahih. Na kuhusiana na Ali Ibn Abi Talib na Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhum* basi kama Hadithi hii si sahih kwao wao basi ni sahih kwa Mtizamo wa Masahaba wengineo *Radhi Allahu Anhum*, na hakuna Wajibu wa kua Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wanatakiwa wawe wanazijua Hadith zote za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.'***

Hivyo kulingana na Mtizamo wa Watu wa Morocco Madhhab ya Imam Malik basi ni kua kama Mtu akigusa sehemu zake za Siri basi anatakiwa atie Udhu kama akiwa hajasali bado, lakini kama ikiwa ameshasali basi itambidi airudie Sala yake hio ndani ya Wakati wake.

Hivyo Mtu akigusa sehemu za Siri kwa Tumbo la Kiganja au kwa Vidole bila kuwepo kizuizi basi itamuwajibikia kutia Udhu, na hio ni kulingana na Mtizamo wa Imam Ibn Qasim Al Maliki pia.' *(Al Dhahiirat)*

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Nujaym Al Hanafi basi amesema kuhusina na Hadith ya Talq Ibn Ali *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Hadith ya Talq haiwezekani kua imebatilishwa kwa sababu ina Ta'alil ndani yake yaani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitumia Qiyas na kutoa Fatwa kua ni sawa na kugusa sehemu nyenginezo za Mwili, hivyo Hadith hio haiwezekani kua imebatilishwa'***(Mi'raj al-Dirayah)**

Kwa upande mwengine basi tunaona kua anasema Imam Ibn Al Hummam Al Hanafi kua: '**Mbali ya kua hadith mbili hizi zinapingana lakini ni Hasan Hadith, na Hadith ya Talq ina nguvu kuliko Hadith Bushra kwa sababu Hadith ya Talq imenukuliwa na Mwanamme, wakati Bushra ni Mwanamke, yaani Wanaume hua na Umakini wa Kumbukumbu na ndio maana Ushahidi wa Mwanamme mmoja hua ni sawa na Ushahidi wa Wanawake wawili.**'*(Fat-h Al Qadir Imam Ibn Al Hummam)*

Hivyo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wanakubaliana kama anavyosema Imam Ibn Nujaym kua: **'Na kugusa Sehemu za Siri za Mwanamme au Mwanamke hua hakunatilishi Udhu hata kama ikiwa kugusa huko ni bila ya Kizuizi'(***Al Bahr Al Raiq)*

Na hivyo ndivyo pia ilivyosemwa kwenye Umdat Al Riaayah aala Sharh Wiqaya,Durr Al Mukhtar, Fatawa Al Hindiyyah, Al Hadiyat Al Aaliyah, Maraqi Al Falah na Durar Al Hukam.

Na uthibitisho wao unasimamia pia kwenye Hadith ya Mulazim Ibn Amar ambae amesema kua amesema Abd Allah Ibn Bandar kua amesema Qays Ibn Talq Ibn Ali kua amesema Baba yake kua **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa kuhusiana na Mtu aliejigusa sehemu zake Siri nae akasema kua Jee hio si sehemu ya Mwili wako?'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Tahawi Al Hanafi basi amesema kuhusiana na Hadith hii kua: **'Mnyororo wa walionukuu Hadith hii ni sahih na hakuna kasoro katika Isnad yake wala Matn (Maneno) yake'***(Nasb Al Rayah)*

Na Imam Al Zaylai pia amenukuu hadith nne zenye Minyororo ya walionukuu ambao ni watu tofauti ikiwemo ile isemayo kua: **'Amesema Abu Umamah Al Bahil kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliuliuzwa kuhusian na Kugusa sehemu za Siri na akajibu kwa kuuliza kua : Kwa Hakika Hizo ni sehemu ya Mwili wako.(***Tabyin Al Haqaiq)*

Ambapo kwa upande wa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wanaokubaliana na mtizamo huu baada ya Abd Allah Ibn Masud na Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhum* basi Pia Ammar Ibn Yasir, Hudhayfah, Imran Ibn Husayn, Abu Dardaa, Zayd Ibn Thabit Radhi Allahu Anhum. Kwa upande wa Maimamu wa Tabiina ni pamoja na Imam Rabiah, Imam Al Thawry, Imam Ibn Al Mundhir, Imam Hasan Al Basr.

Na imesemwa katika Fiqh Ala Madhhahib Al Arbaa kua: **'Baadhi Ya Wanazuoni wa Hanafi wameitafsiri Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua:**

مَنْ مَسَّ ذَكَرَه فليتوضأ

‘Atakaegusa Dhakar yake basi na Atawadhe’ kua inamaanisha Kutawadha kwa Kilugha yaani kukosha Mikono yake Mtu husika baada ya kugusa kabla ya Kusali, hivyo kugusa sehemu yeyote ya Mwili hua hakubatilishi Udhu.

Hivyo kama Mtu atajigusa sehemu zake za Siri za Haja Kubwa basi hautobatilika Udhu wake, napia kwa upande wa Mwanamke kama akijigusa katika sehemu zake za Siri za mbele basi Udhu hautenguki. Lakini hata hivyo kama ataingiza kitu ndani yake na kisha akakitoa kwa mfano kama Kidole chote, kidonge cha Pamba chote au Sindano yote n.k basi Udhu utamtoka, kwa sababu Hukmu yake hua ni sawa na mwenye kutokwa na Kitu ambacho kilimuingia ndani yake.

Hivyo kama ikiwa ataingiza sehemu ya kitu hicho kisha akawa hakukitoa, na kisha akakitoa lakini kikawa kimeroa au kina harufu basi Udhu wake utatenguka, lakini ikiwa kikavu na hakina harufu basi Udhu wake hautobatilika.(*Fiqh Aala Madhahib Al Arbaa)***

Kwani ingawa jana tuliahidiana kua tunaingia katika mada ya Kutenguka kwa Udhu kutokana na kugusana kwa jinsia tofauti, lakini kuna masuali ambayo yamejitokeza na hivyo bora kumalizana nayo kabisa. Ambapo Masuali hayo ni kua **Jee Sehemu za Siri za Mtoto Mdogo zinatengua Udhu ama la? Na Jee sehemu za Siri za Wanyama zinatengua Udhu ama la?**

Naam..anasema Qadhi Al Qudhat Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Basr Al Shafii kua: ‘**Ama kuhusiana na Hukmu ya Kuhusa sehemu za Siri za Mtoto mdogo basi amesema Al Shafii *Rahimahumu Allah* kua: Hukmu yake ji sawia kwa Mtu Mzima na Mtoto Mdogo pia.**

Kisha Imam Al Mawardi anaendelea kusema kua: ‘Hii ni kama alivyosema Al Shafii kua hakuna tofauti baina ya sehemu za Siri za Mtu Mzima na za Mtoto Mdogo kuhusiana na kubatilisha kwake Udhu. Ingawa Imam Malik na Imam Al Zuhri wao wanasema kua Udhu haubatiliki kutokana na Kugusa sehemu za Siri za Mtoto mdogo, na hii ni kulingana na Hadith isemayo kua:

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aligusa Dhakar ya Hasan na kisha hakutia Udhu. Na pia ni kwa sababu kuangalia sehemu za Siri za Mtoto hua kinaruhusika, na hivyo Kugusa basi hua hakutengui Udhu kama vile ilivyokua katika kugusa sehemu nyengine za Mwili.**

Na pia kwa Sababu udhu hua Haubatiliki kutokana na Kugusana na Mtoto Mdogo wa Jinsia nyengine, hivyo basi Udhu hua haubatiliki kutokana na kugusa sehemu za Siri za Mtoto.

Lakini hata hivyo kwa upande wetu sisi Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunasimamia kwenye uthibitisho wa Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* iliyosema kua: Yeyote yule atakaegusa sehemu za Siri basi Kutia Udhu ni Lazima.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakutofautisha baina ya sehemu za Siri za Mtoto wala za Mtu mzima, hivyo kugusa sehemu za Siri za Mtoto kunabatilisha udhu kama vile ilivyo kwa Mtu mzima.

Na hivyo kuhusiana na Hadith waliyoinukuu wanaosema kua Hakubatilishi Udhu basi, haina ushahidi wowote, kwa sababu hakuna iliposemwa kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimgusa Mjukuu wake sehemu za Siri kisha akasali kabla ya kutia Udhu.

Hivyo basi hadith hii inachukuliwa kumaanisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*. Alimgusa sehemu za Siri lakini hakutia Udhu hapo hapo baada yake bali alitia Udhu pale aliponyanyuka kutoka katika sehemu aliyokaa na kisha ndio akatia Udhu.

Ambapo kuhusiana na hoja yao ya kua Kwa sababu hua inaruhusika kuangalia sehemu za Siri za Mtoto mdogo basi jibu lake ni kua Kila kinachobatilisha Udhu hua kinahusiana na kuruhusika kwake na kukatazwa kwake.

Hivi Jee hawaoni kua Udhu unabatilika kwa kugusa?na hivyo hakuna tofauti baina ya Kumguaa Mke wako na kumgusa Mwanamke mgeni kwako.

Ama kuhusiana na Hoja ya Kugusana na Mwanamke asiekua Mwari hakubatilishi Udhu lakini sisi kwa upande wetu tuna mitizamo miwili juu yake ambapo wa kwanza ni kua Kunabatilisha na Mtizamo wa pili ni kua Hakubatilishi.

Na Tofauti baina ya miguso hio ni kua kugusa sehemu za Siri hua ni kubaya zaidi kiuzito kuliko kugusa kwa Mguso wa sehemu nyenginw za Mwili.

Kwani Jee hamuoni kua Ili udhu ubatilike kutokana na kugusana basi hua ni lazima iwe kwa Jinsia tofauti yaani baina ya Mwanamme na Mwanamke, lakini haiwi baina ya jinsia moja yaani Mwanamme kwa Mwanamme, au Mwanammke kwa Mwanamke?

Hivyo Hukmu hii hii ya kugusa sehemu nyengine za mwili pia inatumika kwa Mtu mzima na Mtoto pia.

Na ingawa hali iko hivyo lakini kwa upande wa kugusa sehemu za Siri hali ni tofauti kwani hakuna kutofautisha kua kuhusa sehemu za Siri hizo iwe baina ya Mwanamme na Mwanammke, Mwanamme na Mwanamme au Mwanamke na Mwanamke, Mzee au Mdogo, au Mtu mwenyewe peke yake hua kote kunabatilisha Udhu.

Kwa maana hio basi Kama Mtu atakua hakutahiriwa na kisha akajigusa sehemu ya siri ambayo haikutahiriwa bado, basi Udhu wake utabatilika, lakini kama ikiwa ataigusa sehemu ya kipande kilichokatwa na kiko peke yake tofauti na mwili wake basi hua si sehemu yake ya Siri na hivyo hakutobatilisha Udhu wake.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Imam Al Mawardi anasema kuhusiana na kugusa sehemu za Siri za Mnyama kua: **'Imam Al Shafii anasema kua Kugusa sehemu za Siri za Mnyama hakubatilishi Udhu, na huu ndio Mtizamo wake katika vitabu vyake vyote.**

Na amesema Al Layth Ibn Saad kua Kugusa sehemu za Siri za Mnyama kunabtilisha Udhu, na Ataa amesema hivyo pia, Lakini Mitizamo hii sio Sahih, na hii ni kwa sababu hakuna Wajibu wa Kua lazima Mnyama ahifadhiwe sehemu zake za Siri.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Na huo ndio pia Mtizamo wa Imam An Nawawi katika Al Majmuu kua hakubatilishi Udhu.

Na amesema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni ni kua Kugusa sehemu za Siri za Mnyama hakubatilishi Udhu.'***(Al Mughni)*

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA UDH KWA KUGUSANA NA JINSIA NYENGINE.

❖❖❖❖

Kwani miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambae ni mwenye kua na Sifa ya As-hab Al Wujuh yaani Watu wenye Kuainisha, Sura, Uso au Muonekano mkuu wa Fiqh ya Madhab ya Imam Al Shafii basi ni yule aitwae: Al Allamah, Al Faqih, Al Muhaqqiq Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Ali Al Shirazi, Al Firuzibad Al Shafii ambae alizaliwa Nchini Iran katika Mji wa Firuzibad na akafariki katika Mji wa Baghdad mnamo mwaka 1038 C.E/ 476 Al Hijr.

Yaani miaka 30 baada ya Kuzaliwa Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii. Ambapo nami nimeanza nae kwa sababu katika Mada hii ya Kutenguka kwa Sala, na Udhu kutokana na Mtu kugusana na Mtu wa Jinsia nyengine tunaanza na kuchota Kutoka kwenye kina cha Bahari ya Ilm yake kisha ndio tutazama kwenye Bahari za Ilm za Wengineo.

Kwani Mara kadhaa tumekua tukimnukuu Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kutoka katika Kitabu chake cha Al Majmuu Fi Sharh Al Muhadhdhab. Ambacho kinatokana na Kitabu cha Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii kiitwacho Al Muhadhdhab Fii Fiqh Al Imam Al Shafii. Hivyo Al Majmuu cha Imam An Nawawi Al Shafii ni Ufafanuzi wa Al Muhadhdhab cha Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii.

Naam.hivyo anasema Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Ali Al Shirazi Al Firuzabad Al Shafii katika Al Muhadhdhab kua: **‘Ama kuhusiana na Kugusana na Mwanamke basi hua kunabatilisha Udhu Ambapo hii hua ni pale Mwanamme anapogusa ngozi ya Mwanammke au Mwanamke anapogusa Ngozi ya Mwanamme bila ya kuwepo kwa kizuizi baina yake**. **Na Hii ni kutokana na Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema:**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقۡرَبُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنتُمۡ سُكَٰرَىٰ حَتَّىٰ تَعۡلَمُواْ مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغۡتَسِلُواْۚ وَإِن كُنتُم مَّرۡضَىٰٓ أَوۡ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوۡ جَآءَ أَحَدٞ مِّنكُم مِّنَ ٱلۡغَآئِطِ أَوۡ لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمۡ تَجِدُواْ مَآءٗ فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدٗا طَيِّبٗا فَٱمۡسَحُواْ بِوُجُوهِكُمۡ وَأَيۡدِيكُمۡۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَفُوّٗا غَفُورٗا﴾

Ya ayyuha alladhina amanoo la taqraboo alssalata waantum sukara hatta taAAlamoo ma taqooloona wala junuban illa AAabiree sabeelin hatta taghtasiloo wa-in kuntum marda aw AAala safarin aw jaa ahadun minkum mina algha-iti aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban faimsahoo biwujoohikum waaydeekum inna Allaha kana AAafuwwan ghafooran. *(Surat An Nisaa 4:43).*

Tafsir: ***Enyi mlioamini! Msiikaribie Sala wakati mkiwa mmelewa hadi pale mtakapojua maana ya mkisemacho, wala mkiwa katika hali ya janaba isipokua pale mtakapokua safarini (bila ya kua na maji ya kutosha), hadi mtakapokosha mwili wenu wote. Na mkiwa mnaumwa, au mko safarini au mnapoenda haja au mnapo (لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi, kupangusa nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Allah ni mwingi wa kusamehe na msamehevu sana’.*** *(Al Muhadhdhab Fi Fiqh Imam Al Shafii - Imam Al Shirazi)*

Na hatujamalizana na maelezo ya Imam Al Shirazi ila kwanza nataka tufafanue kidogo aya illi tupate

kufahamiana kwa vizuri zaidi. Hivyo kama tunavyoiona Aya kua ni moja kati ya Aya zenye Amrisho la Tayammam ambapo hapo awali tulipozungumzia Tayammam tuliigusa aya hii kwa kifupi kwani tulitumia zaidi aya nyenzake ya Tayammam ambayo ni ya Surat Al Maidah 5:6.

Na hi ni kwa sababu Aya ya Surat Al Maidah imeanza moja kwa moja kwa Kuamrisha kuhusiana na Namna ya kutia Udhu na kisha ndio ikasema juu ya Tayammam Kama yakikosekana Maji. Ambapo aya hii imeanza na katazo la Kutoikaribia Sala huku watu wakiwa Wamelewa. Na hii ni kwa sababu Kutokana na Hikma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hakutaka Kuwafanyia Ugumu Wafuasi wa Dini ya Kiislam ambayo ilikua ndio kwanza inaingia kwa Mfumo wa Maisha ya Watu.

Hivyo kutokana na Hikma zake basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* alikua anajua kua Watu walikua Wanalewa, hivyo ili kuwakataza basi kwanza alitaka kuwaonesha Madhara na Athari za Ulevi kua unaweza ukasema kitu kisha ikawa hujui umesema nini, kwa sababu unapolewa akili hua si yako tena.

Kwani anasema Abd Rahman kua**: 'Siku Moja Abd Rahman Ibn Awf alitayarisha chakula na kuwaalika Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, hivyo Wakala na wakanywa, na mara ikaingia wakati wa Sala ya Magharibi, hivyo Wakasimama na Kusali, na Mmoja akawa Imam na akasoma Surat Al Kafirun, lakini akaisoma aya ya pili isemayo *La aAabudu MataAabuduna* bila ya kutamka Neno *La* ambalo ni la mwanzo ni mwa aya yaani akasema *aAabudu MataAabuduna* hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha aya hii.'***(Asbab Al Nuzul Al Wahidi)***

Hivyo sehemu ya kushushwa kwa aya hii ilikua kama Tahadhari kua sawa kunyweni, lakini hakikisheni kua Mnapotaka kusali basi muwe hamjalewa, yaani muwe na akili zenu timamu huku mkijua mkisemacho na mpate kuzingatia ndani ya Sala zenu. Na daada ya Aya hii kuteremshwa, walikuwa wakiepuka ulevi wakati wa nyakati za Sala mpaka Aya ya uharamu wa ulevi ilipoteremka baada ya watu kuzoeazoea kuacha kulewa ndio *Allah Subhanah wa Taala* akashusha Aya ya Kuharamisha kabisa Ulevi ambazo ni aya ya Surat Al Baqara 2:219 isemayo:

﴿يَسْأَلُونَكَ عَنِ ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ قُلْ فِيهِمَآ إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَإِثْمُهُمَآ أَكْبَرُ مِن نَّفْعِهِمَا وَيَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنفِقُونَ قُلِ ٱلْعَفْوَ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ ٱللَّهُ لَكُمُ ٱلآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ﴾

Yas-aloonaka AAani alkhamri waalmaysiri qul feehim<u>a</u> ithmun kabeerun waman<u>a</u>fiAAu lilnn<u>a</u>si wa-ithmuhum<u>a</u> akbaru min nafAAihim<u>a</u> wayas-aloonaka m<u>adha</u> yunfiqoona quli alAAafwa ka<u>dha</u>lika yubayyinu All<u>a</u>hu lakumu al-<u>aya</u>ti laAAallakum tatafakkaroona

Tafsir: ***Wanakuuliza (Ewe Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam) kuhusiana na Ulevi na Kamari, Waambie kua: 'Ndani yake Kuna Dhambi Kubwa sana, na baadhi ya manufaa kwa Watu, lakini Dhambi zake ni kubwa kuliko Manufaa yake' na wanakuuliza kuhusiana na kile wanachostahiki Kutoa Waambie kua: 'Kile cha ziada wasichokihitajia' Hivyo ndivyo Allah anavyokubainishieni Sharia zake ili mpate kutafakkari.***

Na katika Surat Al Maidah 5:90.

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡخَمۡرُ وَٱلۡمَيۡسِرُ وَٱلۡأَنصَابُ وَٱلۡأَزۡلَٰمُ رِجۡسٞ مِّنۡ عَمَلِ ٱلشَّيۡطَٰنِ فَٱجۡتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo innama alkhamru waalmaysiru waal-ansabu waal-azlamu rijsun min AAamali alshshaytani faijtaniboohu laAAallakum tuflihoona.

Tafsir: ***Enyi Mlioamini! Hakika ya Vilevi, Bahati Nasibu, Vyano Vya Kafara na Al Azlamu (Vitumikavyo katika kubashiria juu ya bahati au kufanya maamuzi) ni Upotovu wa miongoni mwa Amali za Shaytani, Hivyo jitengeni navyo ili mpate kua wenye kunufaika.***

Naam..hivyo anasema Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Ali Al Shirazi Al Firuzabad Al Shafii katika Al Muhadhdhab kua**: 'Ama kuhusiana na Kugusana na Mwanamke basi hua kunabatilisha Udhu. Ambapo hii hua ni pale Mwanamme anapogusa ngozi ya Mwanammke au Mwanamke anapogusa Ngozi ya Mwanamme bila ya kuwepo kwa kizuizi baina yake. Na Hii ni kutokana na Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema kua:**

﴿أَوۡ لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمۡ تَجِدُواْ مَآءٗ فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدٗا طَيِّبٗا﴾

Aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban *(Surat An Nisaa).*

Tafsir: ***Au mnapo (لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi,*** *(Al Muhadhdhab Fi Fiqh Imam Al Shafii - Imam Al Abu Is-haq Al Shirazi)*

Ambapo juu ya kuhusiana na Alieguswa basi kuna Mitizamo miwili juu yake. Mtizamo wa Kwanza ni kua Udhu Unabatilika. Na hii ni kwa sababu Ni mguso wa baina ya Mwanamme na Mwanammke ndio unaobatilisha Utohara wa Yule alieguswa. Hivyo Udhu wa Yule alieguswa Hubatilika, kama vile unavyobatilika Udhu kutokana na Kuingiliana Kimwili, kwa yule alieingiliwa pia.

Na pia kuna Mtizamo wa kua Haubatiliki kwa sababu Aisha *Radhi Allahu Anha* Amesema katika Hadith kua: 'Nilimkosa mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nilipoamka Kitandani na hivyo nikanyanyuka na kumtafuta. Na hivyo mkono wangu ukagusa Nyayo yake, na hivyo baada ya Sala akaniuliza Jee Shaytani wako Alikuzidi?'

Hivyo Kama ikiwa Udhu wa Mtu anaeguswa Unabatilika basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angekata Sala yake. Na kwa kua Kugusa kunabatilisha Udhu basi Udhu wa yule aliegusa ndio unabatilika na wala sio wa yule alieguswa yaani hii hua sawa na Mtu mwenye Udhu kisha akagusa Sehemu za Siri za Mwenzake.

Na hivyo kama ikiwa Mtu Mwanamme atagusa Nywele au Kucha za Mwanammke basi hautobatilila Udhu wake kwa sababu ya kua hapati hisia za Raha kutokana na kugusa vitu hivyo bali hupata hisia za Raha kutokana na kuagalia tu vitu hivyo. kama Mtu akimgusa yule asieruhusika kumuoa basi kuna Mitizamo miwili juu yake. Ambapo wa kwanza ni kua Udhu Unabatilika na hii ni kulingana na maana ya Aya.

Na Mtizamo wa pili ni kua haubatiliki na hii ni kwa sababu hua hakuna hisia za Matamanio kwa yule asieruhusika kumuoa, hivyo hua ni sawa kwa Mwanamme kugusana na Mwanamme mwenzake au kwa Mwanammke Kugusana na Mwanawke mwenzake.

Ama kuhusiana na Mwanamke mdogo asietamanika kwa Mtu husika na Mwanamke Mzee asietamanika na mtu husika basi kuna mitizamo miwili juu yake. Ambapo kulingana na Mtizamo wa Mjumuisho wa Aya basi Udhu hua Unabatilika. Lakini kutokana na upande mwengine wa kutotamanika kwa Mwanamke husika basi hua hakubatilishi Udhu, na hivyo hua ni sawa na Kugusa Nywele.'*(Al Muhadhdhab Fii Fiqh Al Imam Al Shafii)*

Naam hio ni kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu kwa Kugusa. Na bila ya shaka mtizamo huu ni mwanzo tu wa kuingiza vidole vya Mguu kwenye Bahari ya Mada hii na tumeanza nao kwa sababu baadae tutaurudia kukumbushana kitu muhimu juu yake.

Kwani tunapozungumzia kuhusiana na Mtizamo wa Kutenguka Udhu kwa Mtu mmoja Kugusana kwa Ngozi ya Mtu wa Jinsia Nyengine basi Wanazuoni wametofautiana Sana Juu yake. Na hii ni kwa sababu ya Utofauti wa Ufahamu wa neno (لاَمَسْتُمُ‌ٱلنِّسَآء) *Lamastumu An Nisaa yaani Kugusana na Wanawake* Kama ilivyosema Aya kwani kila mmoja miongoni mwa Wanazuoni wa Skuli za Madhhab amesema kulingana na maana yake. Na hii pia ni kulingana na Mtizamo wa Maana ya neno Lamas kama linavyotumika kikawaida, Kihadith na pia kulingana na matumizi yake katika aya Tofauti ndani ya Qur'an kama tutakavyoona katika Ufafanuzi wake. Inshaa Allah

Hivyo Mtizamo wa Kwanza kuhusiana na Kutenguka kwa Udhu kutokana na Kugusana Ngozi kwa Ngozi baina ya Jinsia mbili Tofauti ni kua Kunabatilisha Udhu. Ambapo hii ni kama tulivyoona kwenye Utangulizi kulingana na mtizamo wa Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii ambao hata hivyo kwa kua Mtizamo huu unatakiwa kufafanuliwa kwa kina kulingana na Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi tutaachana nao kwanza hadi pale tutakapomalizia kuangalia Mitizamo iliyobakia Ya Madhhab mengine.

Na miongoni mwao basi ni Mtizamo wa Pili ambao ni Mtizamo wa Wanafiqh wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal ambapo wao wanasema Kua: '**Kugusana kwa Ngozi ya Mtu mmoja kwa Ngozi ya Mtu mwengine mwenye Jinsia tofauti basi hua kunategemeana na hali ya mguso husika. Kwani kama ikiwa Mguso huo si wenye kua na hisia za Matamanio ndani yake basi Udhu hua hautenguki.**

Ambapo ndani yake Mtizamo huu kuna Kugusa kwa kukusudia na kwa hisia na kutokusudia, hivyo kama ikiwa ni kwa kukusudia na kwa matamanio basi Udhu hutenguka, lakini vyenginevyo hua hautenguki.

Na kisha kuna Mtizamo wa Tatu ambao ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Fiqh ya Skuli ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambao wao Wanasema kua: '**Kugusana kwa Ngozi ya Mtu mmoja kwa Ngozi ya Mtu mwengine mwenye Jinsia tofauti basi hua kunatengua Udhu kama ikiwa tayari wahusika wanataka kuingiliana kimwili.'**

Ambapo kwa Upande wa Imam Muhammad Ibn Hassan Al Hanafi basi yeye anasema kua: 'Kugusana na Mwanamke hakutengui Udhu bali kinachotengua Udhu ni kitendo cha Aibu kinachojumuisha kugusa Uke.'

Hivyo kwa kua kuna mitizamo tofauti juu yake basi tunaanza na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambao wao wanasema kua: '**Unapokua na Shaka basi Mfuate Sarkhasi.'**

Ambapo Sarkahsi si Mwengine yeyote isipokua ni yule Imam Mujtahidiin Al Masail wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa aliezaliwa mnamo mwaka 400 Al Hijra katika Mji wa Sarakhs uliokua katika ardhi ya Khurasan. Na alikua akiitwa Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Sahl Abu Bakr Shams Al Aimah Al Sarkhasi Al Hanafi. Mujtahidin Al Masail Shams Al Aimah Imam Al Sarkhasi alifariki mnamo mwaka 483 Al Hijra.

Hivyo Shams Al Aimah Al Sarkhasi Al Khurasan Al Hanafi anasema kuhusiana na Kutobatilika kwa Udhu kutokana na Kugusana na Mtu wa Jinsia nyengine kua: '**Udhu hautenguki kutokana naKugusana na Wanawake na hata baada ya Kubusiana nae iwe kwa Matamanio au bila ya Kua na Matamanio. Na hii ni kutokana na kua kiasili Udhu hua haubatiliki isipokua kutokana na kitu ambacho kimethibitishwa kutokana na Uthibitisho wa Dhahiri.'***(Kitab Al Mabsut)*

Shams Al Aimah Al Sarkhasi Al Khurasan Al Hanafi amesema tena katika Fat-h Al Qadir kua: **'Udhu hua unahitajika baada kuingiliana Kimwili, na hii inaamisha kua baada ya pande zote mbili kua uchi na kukumbatia, na sehemu zao za Siri kugusana, ambapo kulingana na Muhammad basi ni kua, hautobatilika hadi pale itakapokua mtu ana uhakika kua ametokwa na Madhii, lakini bila ya shaka hu ani bora zaidi kutia Udhu kwa ajili ya Tahadhari.'***(Fat-h Al Qadir)*

Ama kuhusiana na uthibitisho wa Aya isemayo kua:

﴿أَوْ لَـٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدًا طَيِّبًا﴾

Aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban *(Surat An Nisaa 4:43).*

Tafsir: ***Au mnapo (لَامَسْتُمُالنِّسَاء) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi,***

Basi Wanasema Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua **'Neno Lamas hua linamaanisha "Kuingiliana Kimwili" kama vile alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Surat Al Imran kua:**

﴿قَالَتْ رَبِّ أَنَّىٰ يَكُونُ لِي وَلَدٌ وَلَمْ يَمْسَسْنِي بَشَرٌ﴾

Qalat Rabbi Anna Yakuunu Lii Waladu Walam yamsasnii Basharun. (*Surat Al Imran 3:47)*

Tafsir; ***Alisema (Maryam Bint Imran) Mola Wangu****: '**Nitawezaje Mimi kupata Mtoto Wakati Sijaguswa na Mtu'***

Na miongoni mwa Vithibitisho vyao Wanafiqh wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi ni Hadith zenye kuthibitisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aligusana na Wake zake *Radhi Allahu Anhum* wakati akiwa na Udhu na wakati akiwa ndani ya Sala na wala hakukata Sala wala Hakutia Udhu baada ya kugusana nao kabla ya Sala wakati akiwa na Udhu, ambapo miongoni mwao hadith hizo ni kama:

عن عائشةَ قالتْ : كنتُ أنامُ بين يدَيْ رسولِ اللهِ صلَّى اللهُ عليْهِ وسلَّمَ ورجلاي في قبلتِه ، فإذا سجد غمزني ، فقبضتُ رجْلي ، وإذا قام بسطتُهما ثانيًا ، قالتْ : والبيوتُ يومئذٍ ليس فيها مصابيحُ

Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha kua*, Mimi nilikua na kawaida ya kulala mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* huku Miguu yangu ikimuelekea yeye katika upande wa Kibla na Alikua kila anaposujudu hua ananigusa nikaikunja miguu yangu, na aliposimama, nikainyoosha tena. Aisha *Radhi Allahu Anha* Akasema: Hakukuwa na taa katika nyumba wakati huo. *(Sahih Muslim)*

Na amesema pia Aisha *Radhi Allahu Anha* katika Hadith nyengine pia:

فَقَدْتُ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لَيْلَةً مِنَ الْفِرَاشِ فَالْتَمَسْتُهُ فَوَقَعَتْ يَدِي عَلَى بَطْنِ قَدَمَيْهِ وَهُوَ فِي الْمَسْجِدِ وَهُمَا مَنْصُوبَتَانِ وَهُوَ يَقُولُ اللهُمَّ أَعُوذُ بِرِضَاكَ مِنْ سَخَطِكَ، وَبِمُعَافَاتِكَ مِنْ عُقُوبَتِكَ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْكَ لَا أُحْصِي ثَنَاءً عَلَيْكَ أَنْتَ كَمَا أَثْنَيْتَ عَلَى نَفْسِكَ

Siku Moja Usiku sikumuona mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kitandani. Hivyo nikaanza kumtafuta na mara mkono wangu ukaangukia kwenye Nyayo ya Mguu wake akiwa Msikitini, huku nyayo hizo zikiwa zimesimama wima na alikua akisema:
***Allahuma Audhubika Biridhaaka Min Sakhatika* - Ya Allah Najikinga kwa Radhi zako kutokana na Ghadhahu zako.**
***Wa bimuaAafaatika Min Auquubatika* - Na Msamaha wako Kutokana na Adhabu zako**
***Wa Auudhubika Minka* - Na Najikinga Kwako.**
***La Uhsi ThanaaAn Aalayka*- Siwezi kukusifu ipasavyo.**
Anta Athnayt aAlaa Nafsika* -Wewe ni Kama Ulivyojisifu Mwenyewe.(Sahih Muslim)*

Na pia kuna hadit isemayo:

أُخْبُرْنَا ابراهيم بن مُحَمَّد المدينى قَالَ أُخْبُرْنَا معبد بن سابه الحسمى عَن مُحَمَّد بن عَمْرو بن عَطاء عَن عُرْوَة بن الزبير عَن عَائِشَة رَضِي الله عَنْهَا قَالَت قبلني رَسُول الله صلى الله عَلَيْهِ وَسلم وَهُوَ متوضئ ثمَّ صلى وَلم يحدث وضوء

Amesema Ibrahim Ibn Muhammad Al Madini kua amesema Ma'bad Ibn Sabah Al-Hamsi kua ametuambia sisi Muhammad Ibn Amr ibn Ata', kua amesema Urwah Ibn al-Zubayr, kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua kainibusu mimi wakati akiwa katika hali y akua na Udhu na alienda Kusali bila ya kutia Udhu.' (*Al-Hujjah ala Ahl al-Madinah)*

Hivyo katika kukumbushana kuhusiana na Kutenguka kwa Udhu na Sala kutokana na Kugusana na Mtu wa Jinsia Nyengine, na kwa kua kuna mitizamo tofauti juu yake basi tunaanza na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambapo tunaona kua anasema Imam Muhammad Ibn Abd Rahman Ibn Abd Rahim Al Mubarakfuri Al Hanafi katika kitabu chake cha Tuhfah Al Ahwadhi kua:

حدثنا قتيبة وهناد وأبو كريب وأحمد بن منيع ومحمود بن غيلان وأبو عمار الحسين بن حريث قالوا:

حدثنا وكيع عن الأعمش عن حبيب بن أبي ثابت عن عروة عن عائشة رضي الله عنها:
قال أن النبي صلى الله عليه وسلم قبّل بعض نسائه ثم خرج إلى الصلاة ولم يتوضأ،
قال قلت: من هي إلا أنت؟ :فضحكت:

‘**Wamesema Qutaybah, Hanad, Abu Qurayb, Ahmad Ibn Mani, Mahmud Ibn Ghailani na Abu Ammar Al Husayn Ibn Harith kua: Ametuambia sisi Waki’i kua amesema Al Amash kua amesema Habib Ibn Abi Thabit kua amesema Urwa kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akimbusu mmoja kati ya Wake zake, na kisha hutoka na kuenda Kusali bila kutia Udhu’**

Hivyo Habib Ibn Thabit akasema kua: ‘Mimi nikasema: ‘Atakua nani kama si wewe? : Hivyo Aisha *Radhi Allahu Anha* akacheka tu.’

Imam Mubarakfuri anaendelea kusema kua: **‘Amesema Abu Isa At Tirmidhii kua kuna hadith nyengine kama hii zimenukuliwa na zaidi ya Mtu mmoja miongoni mwa wenye Ilm kutokea kwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.* Na miongoni mwa Tabiina basi huu ndio Mtizamo wa Imam Sufyan Ath Thawry.**

Lakini watu wa Kufah basi wao wanasema kua Hakuna Udhu baada ya Kubusiana baina ya Mwanammke na Mwanamme Na Imam Malik Ibn Anas, Imam Al Awzai, Imam al Shafii,Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh kua hakuna Udhu baada ya Kubusiana baina ya Mwanamme na Mwanammke. Na huu ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa wenye Ilm kutoka kwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na Tabiina.

Imam At Tirmidhii ambae ni Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii anaendelea kusema kua **Na Wanazuoni wetu (wa Madhhab ya Imam Al Shafii) wameachana na Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha.* Kuhusiana na Jambo hili kwa sababi ya kua si Hadith Sahih kulingana na vigezo vyao kutokana na Wanukuzi wake. Kwani Nimemsikia mimi Abu Bakr Al Attar Al Basr akisema kua amesema Al Ibn Al Madini kua amesema kua Yahya Ibn Sadi Al Qattani amesema kua Hadith hii ni dhaifu sana na si chochote. Kwani nimemsikia mimi Muhammad Ibn Ismail (Imam Al Bukhari) akisema kua Hii ni Hadith Dhaif.**

Na Habib Ibn Abi Thabit amesema kua Hakusoma Hadith kwa Urwa Na imesemwa kua amesema Ibrahim At Taymi kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akimbusu bila kutia Udhu.

Hii pia si Hadith Sahih, kwani sisi hatujui kuhusiana na Ibrahim At Taymi kua alisoma Hadith kutoka kwa Aisha *Radhi Allahu Anha,* na Hakuna Hadith Sahih kutoka kwa Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam juu ya Jambo hili.’’*(Tuhfah Al Ahwadhi Bi Sharh Jamii Tirmidhii - Imam Al Mubarakfuri)*

Ama kwa upande wa Imam Abu Al Hasan Ahmad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Ahmad Ibn Jafar Al Quduri Al Hanafi katika kitabu chake kiitwacho Al Tajriid ambacho ni chenye Kulinganisha baina ya Hukmu za Skuli ya Fiqh Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Hukmi za Skuli za Madhhab ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kulingana na vithibitisho vya Mitizamo ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa na kujibu hoja kwa kusema kua Wanazuoni wetu wanasema kua**:**

‘Kwa Mwanamme kumgusa Mwanammke hua Hakutengui Udhu. **Na hii ni kwa sababu amesema Sufyan Ath Thawry kua amesema Abu Rawq kua amesema Ibrahim At Taymi kua amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua Akimbusu bila ya Kutia Udhu Hivyo Hoja yao (Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii) kua Ibrahim At Taymi hakuwahi kukutana na Aisha *Radhi Allahu Anha* haina Nguvu kwa sababu kwa Upande wetu sisi *Hadith Mursal* na *Hadith Mutassal* ni sawia.’**

Ambapo kabla ya kuendelea basi tukumbushane kua *Mursal Hadith* hua ni Hadith ambayo haina jina la Sabaha katika kunukuliwa kwake bali ina jina la Tabiin ambae moja kwa moja hunukuu maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na *Mutassal Hadith* hua ni Hadith ambayo kila Anaenukuu hua amenukuu kutoka kwa Mwalimu wake moja kwa moja.

Kwa maana hio basi Hadith iliyotangulia huya ni Hadith Mursal, na hivyo Imam Al Quduri anatoa uthibitisho mwengine wa Hadith hio yenye sifa ya *Hadith Mutassal* kwa kusema: ‘**Kwani Imenukuliwa katika baadhi ya Hadith kua Ibrahim At Taymi amesema kua amesema Baba yake kua Aisha *Radhi Allahu Anha* amesema hivyo.**

Na hadith hii imenukuliwa pia na Yahya Ibn Said Al Qattan ambae Mursal hadith zake ni Sahih kuliko Musnad za wengine kutokana na umakini katika kunukuu kwake.

Hivyo Hadith hii imenukuliwa kupitia katika minyororo ya wanukuzi wengi lakini hata hivyo bado inakosoleka kutokana na Mnyororo wa Upande mmoja wa walionukuu ulioainishwa.’*(Al Tajriid Imam Al Quduri)*

Imam Abu Al Hasan Ahmad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Ahmad Ibn Jafar Al Quduri Al Hanafi katika kitabu chake kiitwacho Al Tajriid ambacho ni chenye Kulinganisha baina ya Hukmu za Skuli ya Fiqh Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Hukmu za Skuli za Madhhab ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kulingana na vithibitisho vya Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anaendelea kusema kua: ‘**Wanazuoni wetu wamesema kuaKugusana na Wanawake hakutengui Udhu kwa sababu Kuna Hadith isemayo pia kua amesema Abd Al Malik Ibn Muhammad kua amesema Hisham Ibn Urwa kua amesema Baba yake kua:**

Amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akimbusu wakati akiwa amefunga na kusema: Busu halibatilishi Udhu wala halibatilishi Funga Ewe Humayra! Kuna wepesi katika Dini.’*(Sunnan Abu Daud)*

Rasul Allah Salallahu Alayhi Wa Salam alikua akimuita Aisha *Radhi Allahu Anha* pia kwa Jina la kimapenzi la Humayra. Neno Humayra kwa Kilugha hua linamaanisha Mwanammke Mweupe mwenye Mashavu mazuri meupe yaliyovilia wekundu kwa mbaali.

Imam Al Quduri anaendelea kusema kua:

حدثنا محمد بن بشار حدثنا يحيى وعبد الرحمن قالا حدثنا سفيان عن أبي روق عن إبراهيم التيمي عن عائشة رضي الله عنها قال أن النبي صلى الله عليه وسلم قبلها ولم يتوضأ

‘**Amesema pia Muhammad Ibn Bashr kua wamesema Yahya na Abd Rahman kua: Ametuambia Sisi Sufyan kua amesema Abu Rawq kua amesema Ibrahim Al Taymi kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akimbusu bila kutia Udhu.’***(Sunnan Abu Daud)***

Imam Abu Daud anasema kua: ‘Hivi ndivyo al Firyabi alivyokua akiinukuu hadith hii ambayo ni Mursal Hadith’

Imam Al Quduri anaendelea kusema kua: ‘Hadith ya Aisha Ni Sahih lakini mnyororo wa Walioinukuu ni Dhaifu, kutokana na kukatika kwake kwani Ibrahim At Taymi ni Mtoto wa Yazid na hakusikia Hadith kutoka kwa Aisha *Radhi Allahu Anha,* na Yahya ni mtoto wa Said Al Qahtan, Abd Rahman ni Mtoto wa Mahdi na Abu Ruuq ni Atiyah Ibn Al Harith.

Na Imam An Nasai ameinukuu Hadith hii katika Sunan Al Kubra na katika Al Mujtaba kupitia kwa Yahya Al Qatani kwa Mnyororo huu huu wa walionukuu na kisha Imam An Nasai akasema katika *Al Mujtaba* kua: ‘Hakuna Hadith nyengine Nzuri zaidi ya Hii kiuhusiana na Mada hii hata kama ikiwa ni Hadith Mursal.’

Ama kuhusiana na Kugusa basi Kama Mume akimgusa Mkewe kwa hamu na Mapenzi au bila ya Hamu, iwe kwenye Uke Wake au sehemu nyengine yeyote ile ya mwili bila ya Kizuizi na bila ya Kupapasa kwa mguso wake basi Udhu wake hautobatilika kama ilivyosemwa kwenye *Al Bahr Al Raiq Sharh Kanza Al Daqaiq.*

Na imesemwa kwenye Durr Al Mukhtar na Radd Al Mukhtar ya Imam Ibn Aabidin kua: ‘Kugusana na Ngozi ya Mwanammke hakubatilishi Udhu kwa haoi yeyote ile iwe kwa Matamanio ama la.’

Na kuhusiana na Aya isemayo: *Aw Lamastumun Al Nisaa* yaani Au Mtakapogusana na Mwanammke Ambapo Kuhusa hua ni kwa Kutumia Mkono basi Wanazuoni wetu wana mitizamo tofauti:

Mtizamo wa kwanza ni ule wa Wanazuoni wa Ilm ya Kanuni za Fiqh kwa mfano kama Imam Fakhr Al Islam Al Bazdawi ambae amesema kua: ‘Kugusa kwa kawaida hua kunatokana na Mikono, wakati kuingiliana kimwili hua ni Mithilisho, ambapo hata hivyo kuna kukubaliana kwa Wanazuoni wetu juu ya kusudio la Mithilisho la Kuingiliana kimwili kutokana na kua Aya inaruhusu asiekua tohara Kufanya Tayammam na hivyo basi Maana ya Lamastumun kumaanisha kugusa hua inabatilika kwa sababu haiwezekani kwa maana zote mbili kutumika kwenye Aya Moja.

Pili ni kama illivyotajwa kwenye baadhi ya Vitabu vya Fiqh kua kama Kugusa kunajumuishwa na Mwanammke basi hii inamaanisha ni Kuingiliana kimwili ambako kunaungwa mkono na Ukweli wa kua Kugusa hua ni kitendo cha kugusana kinachotokea baina ya Watu wawili au zaidi, na hivyo basi kuhusa hua si lazima Kwa pande zote.

Na Tatu ni kua Lamastumun hua kunajumuisha Kugusa kwa mikono na kuingiliana Kimwili, hivyo sisi tumetafsiri kua ni kuingiliana kimwili. Na amesema Imam Abu Hanifa kuhusiana na Mtu atakaembusu Mwanamke wakati akiwa katika hali ya kua na Udhu, basi Udhu wake hautobatilika.’*(Al Tajriid)*

Na amesema Imam Abd Rahman Al Jazari katika *Kitab Fiqh Ala Madhdhahib Arbaa* kua: **'Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab Ya Imam Abu Hanifa wanasema kua: Kugusa sehemu yeyote ya Mwili hua hakubatilishi Udhu,hata kama Mgusaji na Mguswaji watakua Uchi. Hivyo kama Mume na Mke watatia Udhu na kisha kulala kitandani huku wakiwa hawana nguo na wakagusana basi Udhu wao hautobatilika isipokua kwa Hali mbili zifuatazo:**

Kwanza kama watatokwa na Kitu katika sehemu zao za Siri kama Madhii n.k.

Pili ni kua kama ikiwa hakuna kitu kinachozuia Joto lao la Mwili kufikiana baina yao.

Hivyo kama hakuna kizuizi Kitakachozuia Hisia za Joto la Mwili baina yao kufikiana basi Udhu wa Mwanamke utabatilika hapo hapo ambapo kwa upande wa Udhu wa Mwanamme basi utabatilika baada ya kusimama Uume wake.

Hivyo Kama Mwanamke na Mwanamke watalala pamoja bila ya Nguo na Joto la Miili yao likawa linahisiwa na miili yao basi Udhu wao utatenguka.

Lakini kama ikiwa Mwanamme atamgusa Mwanamme mwenzake wakati wakiwa katika Mabafu ya Jumuia wanakoga basi Udhu hautotenguka isipokua pale mgusaji itakapokua umesimama Uume wake.

Na hivyo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wao huhesabu kutenguka kwa Udhu kwa kugusana huweza kutokea pale itakapokua kuna Nia inayotokana na hisia za Matamanio ya kuingiliana ndani yake.'*(Kitab Al Fiqh aAla Madhahib Al Arbaa)*

Na baada ya kuangalia Mtizamo wa Wanazuni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi tunahama katika Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik kupitia kwa Imam Ahmad Ibn Muhammad Ad Dasuqi Al Maliki katika Kitabu chake kiitwachwo Sharh Al Kabir Al Shaykh Al Dardir wa Khashiyat Al Dasuqi ambacho kinasema kua:

'Na jambo la Pili hua ni Mguso wa Mtu mzima na wala si wa Mtoto hata kama atakua ni Kijana hua hakubatilishi Udhu, kwani Kuingiliana nae kimwili ndio sehemu ya Kugusa, hivyo Udhu Utabatilika kwa kuingiliana nae. Hivyo Kama ukigusana na Mtu wa Jinsia nyengine bila ya kua na Matamanio kama vile Mtu ambae huwezi kumuoa basi Udhu wako haujabatilika.

Kwani Kugusa hua ni Kupata Hisia za Kuhisi kile kinachotakiwa kuhisikana na hisia za Mwili kama Joto au Baridi, Ugumu au Ulaini, au Kujua Uhalisia wa Maumbile ya Kitu kama vile kutaka kujua Kiumbe husika kama ni Mtu ama la.

Na imesemwa iwe kwa Mtu Mzima wala si Mtoto kwa sababu Mguso Hubatilisha Udhu kutokana na Mguso husika kupelekea Kutokwa na Madhii na Mtoto hua hatokwi na Madhii.

Lakini Kama ukigusana na Mtu ambae unaweza kuoana nae kama Mumeo au Mkeo au Mtu mwengine yeyote unaeweza kuoana nae basi hali ya Udhu wako itakua katika Hali zifuatazo kulingana na tukio husika:

1-Kama Mtagusana kwa nia ya Kutamaniana na Mkatamaniana basi Udhu Utabatilika.

2-Kama Mtagusana kwa Nia ya Kutamaniana lakini hamkufanikiwa Kupata hisia za Matamanio basi Udhu Utabatilika.

3-Kama Mkigusana kwa Bahati mbaya lakini Mtu akapata hisia za Matamanio basi Udhu wa Mhusika Utabatilika.

4-Kama Mtagusana bila ya Kua na Nia ya Kiamaniana na hamkutamaniana basi Udhu hautobatilika.

Ambapo inapozungumziwa kuhusiana na Mguso wa Hisia za Matamanio basi hua ni wenye kuanzia kwenye Mabadiliko ya Mapigo ya Moyo na kuingia kwenye kutokwa na Madhii.

Na inapozungumziwa kuhusiana na aina ya Mguso basi hua inahesabiwa kugusa sehemu yeyote ile ya Mwili wa Mtu wa Jinsia nyengine iwe Ngozi, Nywele n.k Kucha, bila kujali kama sehemu husika imefunikwa na kizuizi ama la, kwani ikiwa kuna Nia ya Matamanio au yakatokea Matamanio hata bila kukusudia basi Udhu utabatilika.'*(Sharh Al Kabir Aala Shaykh Ad Dardir wa Khashiyah Ad Dasuqi)*

Imam Ahmad Ibn Muhammad Ad Dasuqi Al Maliki anaendelea kusema katika Kitabu chake kiitwachwo *Sharh Al Kabir Al Shaykh Al Dardir wa Khashiyat Al Dasuqi* kua: '**Ama kuhusiana na Kubusiana Mdomoni basi bila ya shaka hua kunabatilisha Udhu, hata kama ikiwa hakuna Nia ya Matamanio, na hii ni kwa sababu Mdomo ni kiungo chenye hisia zenye kupelekea Kusababisha Matamanio pale itakapokua wanaobusiana ni Watu wazima, au kama ikiwa mmoja miongoni mwao ni Mtu mzima, lakini kama ikiwa vyenginevyo basi hakubatilishi Udhu.**

Na kuhusiana na kubusu kwenye Shavu, au sehemu nyengineyo yoyote ile ya Mwili isipokua sehemu za Siri, basi hua inahesabika kua ni kugusa pia, hivyo hua kunabatilisha Udhu kulingana na Nia ya matamanio.

Kwani Kubusu sehemu za Siri hukmu yake hua ni sawa na Kubusu Mdomoni, yaani hua kunabatilisha Udhu iwe kwa Matamanio ama la, kutokana na kua sehemu hizo ni za Matamanio.

Hivyo kama ikiwa Kubusu huko ni Kubusu kwa sababu ya Kuagana, kwa sababu ya kumuonea Huruma Mgonjwa na kumuonesha Mapenzi na huruma zako kutokana na Mitihani aliyokua nyo Mtu, basi Udhu hautotenguka, isipokua kama yatatokea Matamanio ndani yake basi utatenguka.

Na hata kuangalia kwa mtazamo wa Matamanio pia hua hakutengui Udhu pale itakapokua hakuna Kutokwa na Madhii ndani yake.'*(Sharh Al Kabir Aala Ad Dardir wa Khashiyah Ad Dasuqi Al Maliki)*

Na amesema Imam Abd Rahman Al Jazari katika *Fiqh Aala Madhahib Arbaa* kua: '**Ama Kuhusiana na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi wao Wamesimamia kwenye Msingi unaotokana na Nia ya Matamanio kua ndio inayobatilisha Udhu, hivyo Kugusana na Mtu wa Jinsia nyengine akiwa Mtu mzima mzee hua hajubatilishi Udhu kabisa.**'

Na amesema Imam Malik Ibn Anas kua: '**Kama Ikiwa Mwanammke ataushika Uume wa Mwanamme kwa Matamanio basi Mwanamke huyo itambidi atie Udhu lakini kama ikiwa ameshika bila ya Matamanio, labda kwa sababu ya Udaktari na Mgonjwa n.k basi Udhu hua haubatiliki.**

Hivyo Kama Mwanamke akimgusa Mwanamme kwa Matamanio, au Mwanamme akimgusa Mwanamke kwa Matamanio basi Udhu Utabatilika iwe alieguswa amevaa nguo ama la na kama ikiwa bila ya Matamanio basi hautobatilika.

Na kama Mtu akibusiwa sehemu yeyote isiyokua Mdomoni, wala kwenye sehemu za Siri yaani kama Shavuni, Shingoni, kwenye paji la Uso, Mgongoni n.k bila Matamanio basi Udhu Haubatiliki, lakini kama ikiwa kuna matamanio basi utabatilika.*(Al Mudawwana Al Kubra)*

Naam baada ya Kuangalia Mitizamo ya Wanazuoni wa Skuli za Fiqh za Madhhab ya Imam Abu Hanifa Nuuman Ibn Thabit, na kuangalia Mtizamo wa Wanazuoni wa Skuli ya Fiqh Madhhab ya Imam Malik Ibn Anas kuhusiana na Kutenguka kwa Udhu kutokana na Kugusana na Jinsia nyengine basi na tuangalie Mtizamo wa Wanazuoni wa Skuli ya Fiqh ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Ambapo anasema Muwaffaq Ad Din Abu Muhammad Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Muhammad Ibn Qudamah Ibn Nasr Ibn Abd Allah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Mtizamo unaokubalika zaidi katika Skuli ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ni kua:**

Kugusana na Mwanamke kwa Matamanio hua kunatengua Udhu lakini kugusa hakutengui Udhu isipokua pale itakapokua Kuna Matamanio, Kumgusa Mwanammke kutokana na Matamanio hua Kunabatilisha Udhu,ila kugusa peke yake bila Matamanio hua hakutengui Udhu na hii ni kutokana na mkusanyiko wa Aya na Hadith, kua kitendo cha Kugusa chenyewe hua si Najis na hua kinajitegemea na hivyo kinaweza kua ni chenye kupelekea kugusa Najis.'*(Al Kaafi Fi Fiqh Al Imam Ahmad)***

Na akasema tena Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua '**Na huu ndio Mtizamo wa Imam Al Qaamah, Imam Abu Ubaydah, Imam An Nakhai, Imam Hammad, Imam Malik, Imam Al Thawry, Imam Ash Shabi ambao wamesema kua: Kutia Udhu hua ni Wajibu kwa yule atakaegusa kutokana na Matamanio, lakini hua si Wajibu atakaegusa kutokana na Huruma.'**(Al Mughni)

Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Bahaaudin Al Maqdisi, Shaykh ul Ulamaa Diyaa Ad Din Abu Abd Allah Muhammad Ibn Abd Al Wahid Al Sadi Al Maqdisi Al Hanbal katika kitahu chake cha Al Uddah Sharh Al Umdah.

Na akasema Shaykh ul Hanabil Imam Mansjr Ibn Yunus Al Buhuti Al Hanbal kua: '**Kugusana na Mwanamke kwa Matamanio Hua kunatengua Udhu kwa sababu kufanya hivyo hua ni kwenye kupelekea kuamsha Najis.'***(Rawdha Al Murabi)*

Na mtizamo hua pia ndio wa Imam Abd Al Qadir Ibn Umar Ash Shaybani Al Hanbali katika Kitabu chake cha Nayl Al Maarib. Na pia ndio wa Imam Mari Ibn Yusuf Al Karni Al Hanbali katika kitabu chake cha *Dalil At Talib.*

Na tunapoangalia Ufafanuzi wa Al Muhadith Imam Muhammad Ibn Ali Al Shawkani Al Yamani Al Hanbali, ambae kabla ya Kuingia kwenye Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kwa upande wa Kisalafi basi alikua ni Mfuasi wa Madhhab ya Shia Zaydiyah ya Yemen. Hivyo anasema Imam Al Shawkani kua: *'**Amesema Allah Subhanah wa Ta'ala kua:***

﴿أَوۡ لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمۡ تَجِدُواْ مَآءٗ فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدٗا طَيِّبٗا﴾

Aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban *(Surat An Nisaa 4:43).*

Tafsir: ***Au mnapo (لَامَسْتُمُالنِّسَآء) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi,***

Ambapo pia maneno اة لامستم النساء yalikua pia yakisomwa kama او لمسثم النسء na baadhi ya Masahaba *Radhi Allahu Anhum.* Ambapo amesema Muadh Ibn Jabal *Radhi Allahu Anhu* kua**:**

"جاءَ رَجُلٌ إلى النَّبِيّ صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ فقال: إنِّي عالجَتُ امرَأةً"، معنى عالجَها أي: داعَبَها واستَمتَعَ بها كما يَفعَلُ الرَّجُلُ مع امرَأتِه، "في أقصَى المدينَةِ" في أطرافِها، "وإنِّي أصَبتُ منها ما دونَ أنْ أمَسَّها"

'Kuna Mtu alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kusema: Ya Rasul Allah, Jee unasemaje kuhusiana na Mtu aliekutana na Mwanamke katika mipaka ya Mji na Kumkumbatia, akambusu, na akamchezea kila sehemu na kumfanya kila kitu kama amfanyavyo Mke wake, bila ya kumuingilia?'

(Ambapo neno kumuiingilia illiyotumiwa na hadith hii ni Amassaha linalotokana na neno Lamas lililotoa pia neno Lamastum tunalolielezea)

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakaa Kimya bila kusema kitu, na hivyo *Allah Subhanah wa Ta'ala* akashusha aya isemayo:

﴿وَأَقِمِ الصَّلَاةَ طَرَفَيِ النَّهَارِ وَزُلَفًا مِّنَ اللَّيْلِ ۚ إِنَّ الْحَسَنَاتِ يُذْهِبْنَ السَّيِّئَاتِ ۚ ذَٰلِكَ ذِكْرَىٰ لِلذَّاكِرِينَ﴾

Waaqimi alssalata tarafayi alnnahari wazulafan mina allayli inna alhasanati yuthhibna alssayyi-ati thalika thikra lildhdhakireena. *(Surat Hud 11:114)*

Tafsir: ***Na Simamisheni Sala Katika Mwisho Miwili ya Siku Na Baadhi ya Wakati wa Usiku(yaani Sali Vipindi vitano kwa siku) Kwani kwa Hakika Mambo Mema Huyafuta Maovu Huo ni Ukumbusho kwa Wanaokubali ukumbusho.***

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwiambia Mtu huyo kua Tia Udhu kisha Usali *(Imam Ad Daraqutni)*

Ambapo Hadithi hii imenukuliwa na Imam Al Tirmidhii, Al Hakim na Imam Al Bayhaqi Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Arabi basi yeye ameinukuu Hadith hii pia kutoka kwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kama ilivyosema Hadith isipokua Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ameendelea kusema kua:

"جاءَ رَجُلٌ إلى النَّبِيّ صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ فقال: إنِّي عالجَتُ امرَأةً"، معنى عالجَها أي: داعَبَها واستَمتَعَ بها كما يَفعَلُ الرَّجُلُ مع امرَأتِه، "في أقصَى المدينَةِ" في أطرافِها، "وإنِّي أصَبتُ منها ما دونَ أنْ أمَسَّها"

قال ابنُ مسعودٍ رضِيَ اللهُ عنه: "فقال له عُمَرُ: لقدْ سَتَرَكَ اللهُ"؛ "لو سَتَرتَ على نَفْسِكَ"

Mtu mmoja alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kuna Mtu alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kusema: Ya Rasul Allah, Mimi nimekutana na Mwanamke katika mipaka ya Mji na Kumkumbatia, akambusu, na akamchezea kila sehemu na kumfanya kila kitu kama amfanyavyo Mke wake, lakini hakumuingilia.'

Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* anasema kua; Umar akamwambia, "Allah amekuficha laiti ungejificha wewe mwenyewe. *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakumjibu. Yule mtu akaondoka, na ikashushushwa Aya ifuatayo:

﴿وَأَقِمِ الصَّلَاةَ طَرَفَيِ النَّهَارِ وَزُلَفًا مِّنَ اللَّيْلِ ۚ إِنَّ الْحَسَنَاتِ يُذْهِبْنَ السَّيِّئَاتِ ۚ ذَٰلِكَ ذِكْرَىٰ لِلذَّاكِرِينَ﴾

Waaqimi alssalata tarafayi alnnahari wazulafan mina allayli inna alhasanati yuthhibna alssayyi-ati thalika thikra lilththakireena. *(Surat Hud 11:114)*

*Tafsir: **Na Simamisheni Sala Katika Mwisho Miwili ya Siku Na Baadhi ya Wakati wa Usiku(yaani Sali Vipindi vitano kwa siku) Kwani kwa Hakika Mambo Mema Huyafuta Maovu Huo ni Ukumbusho kwa Wanaokubali ukumbusho.***

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamtuma mtu baada yake, akamwite yule Mtu na alipokuja akamsomea aya :**

﴿وَأَقِمِ الصَّلَاةَ طَرَفَيِ النَّهَارِ وَزُلَفًا مِّنَ اللَّيْلِ ۚ إِنَّ الْحَسَنَاتِ يُذْهِبْنَ السَّيِّئَاتِ ۚ ذَٰلِكَ ذِكْرَىٰ لِلذَّاكِرِينَ﴾

Waaqimi alssalata tarafayi alnnahari wazulafan mina allayli inna alhasanati yuthhibna alssayyi-ati thalika thikra lildhdhakireena. *(Surat Hud 11:114)*

*Tafsir: **Na Simamisheni Sala Katika Mwisho Miwili ya Siku Na Baadhi ya Wakati wa Usiku(yaani Sali Vipindi vitano kwa siku) Kwani kwa Hakika Mambo Mema Huyafuta Maovu Huo ni Ukumbusho kwa Wanaokubali ukumbusho.***

Abd Allah Ibn Masud Radhi Allahu Anhu anaendela kusema kua:

"فقال رَجُلٌ من القَومِ: هذا له خاصَّةً؟ فقال النَّبيُّ صلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ: "بل للنَّاسِ كُلِّهم عامَّةً

Mtu mmoja miongoni mwa watu akasema: Hii ni kwa ajili yake makhsusi. Na akasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: "Bali ni kwa ajili ya watu wote kwa ujumla," maana yake: inawajumuisha wote, naye ni mmoja wao. *(Ahkami Al Qur'an)*

Ambapo maana ya Hadith hii ni kua Miongoni mwa njia zinazomsaidia mtu kutubu—pamoja na kujuta kwa kitendo hicho na kujiepusha kabisa na dhambi—ni kujitahidi kuzidisha na kuzidisha matendo mema mpaka yatawale maisha na moyo wake. Miongoni mwa njia kubwa zaidi ya hizo zinazofuta madhambi ni maombi ya Dua.

Naam..tunarudi kwa Imam Al Shawkani ambae anaendelea kusema baada ya kuelezea Hadith hii kua:
Hivyo uthibitisho wa hadith na aya ya Tayammam hua zinatumiwa pia kama Uthibitisho kwa wale wasemao kua: Kugusana na Mwanamke kunabatilisha udhu wa Mwanamme. Ambapo huu ni Mtizamo wa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu*

***Anhu,* Imam Az Zuhri, na Imam Al Shafii Na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii pamoja na Zayd Ibn Aslam na wengineo.**

Ambapo kwa upande wa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Ataa, Tawus, Abu Hanifa, Abu Yusuf basi wao wote wanasema Kugusana na Mwanamke Hakutengui Udhu.

Na Abu Hanifa na Abu Yusuf basi wao wamesema kua: Isipokua pale Zitakapoguswa sehemu za Siri na zikamwaga Maji yake, na hata kama hayakumwagwa.

Na Wanazuoni wa Kundi la Mwanzo basi wao Wanasema kua Aya Imebainisha wazi kua Kugusana na Jinsia Nyengine hua kunatengua Udhu, na hii inajumuisha kugusa kwa mkono kutokana na neno Aw Lamastum ambalo liko wazi kua ni Kugusa bila kuingiliana kimwili.' *(Nayl Al Awtar)*

Hivyo Imam Al Shawkani Al Hanbali anaendelea kusema kua: '**Kundi la kwanza la Wanazuoni linasema kua Aya imedhihirisha wazi kua Kugusa Jinisia Nyengine ni Kitu kinachopelekea Mtu Kubatilika Udhu wake, na hili linaungwa mkono na Maneno *Aw Lamastumu Al Nisaa* ambako kunamaanisha kugusa Ngozi tu bila kuingiliana Ambapo Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* kugusa Nyayo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kupewa kisingizio cha kama alivyosema Imam Ibn Hajar Al Asqallani katika Fat-h Al Barr kua: 'Inawezekana ikawa kumgusa kwake huko Nyayo ili ni kwa kupitia Kizuizi, au ni kwamba hali hio imerujusika kwa ajili ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* peke yake hua ni kuzidisha Chumvi na kunapingana na maana halisi ya Hadith.**

Na kundi la pili linasema kua, la hapana, bali tunatakiwa kuchukua mfano wa mithili yake kutokana na Uthibitisho wa Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* kuhusiana na Kubusiana na hadithi yake ya kugusa nyayo za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Ambapo hata hivyo hadith ya kubusiana imeshatolewa kasoro ya kua ni Dhaif, na Hadith ya Nyayo imethibitishwa kua ni Mawquf na Marfuu na hali ya Marfu hua ni kiongezo cha kutegemewa Hadith kama wasemavyo Wanazuoni wa Usul.

Na Wanasema Wanazuoni kua Muulizaji Suali katika Hadith ya aliemchezea Mwanamke aliamrishwa Kutia Udhu, na Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* amesema kua Mtu atakaembusu Mke wake au atakaemgusa kwa mkono wake basi ni wajibu kwake kutia Udhu. Na Imam Malik na Imam Al Shafii wameinukuu kutoka kwake, na Imam Al Bayhaqi ameinukuu kutoka kwa Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* ikiwa na maneno yasemayo: 'Kubusu ni sehemu ya Kugusa na Udhu unahitajika baada yake Na kugusa hua ni kudogo kuliko kuingiliana kimwili.'

Na Imam Al Hakim ametoa Uthibitisho wa Hadith kuhusiana na kua kugusa hua ni kudogo kuliko kuingiliana kimwili kulingana na Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae amesema kua: 'Hakuna Siku ya Baridi kali wala Joto Kali isipokua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akija kwetu na Kutubusu na kutugusagusa.'

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Bayhaqi yeye ametoa Uthibitisho wa Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* aliesema kua Zina ya Mkono ni Kugusa, na katika hadith ya Maiz iliulizwa kua Labda Ulibusu au uligusa?

Na kutokana na Hadith ya Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Kubusu ni sehemu ya Kugusa hivyo Tia Udhu baada yake.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuamrisha alieuliza Kutia Udhu kwa sababu ya Labda ni kutokana na Dhambi ndani yake.

Kwani imenukuliwa kua Udhu hua ni sehemu ya Kufutiwa Dhambi Au labda kutokana na kua kwa namna alivyoelezea Mtu huyo juu ya aliyoyafanya na Mwanamke huyo basi yamepelekea kua ni mwenye kuyokwa na Madhii, au pia inawezekana ikawa ni sharti la kuingia kwenye Ibada ya Sala kama ilivyoelezewa na Aya bila kujali kama Udhu wake umemtoka ama la na kutokana na uwezekano huo basi tunaona kua Uthibitisho wake Hadith hii hua unabatilika.

Ama kuhusiana na Hadith ya Ibn Umar na Ibn Masud *Radhi Allahu Anhum* Na alichokisema Imam Al Hakim na Imam Al Bayhaqi, basi hatukatai kutumika kwa mtizamo wa Kugusa kua Unamaanisha Kugusa kwa Mkono, lakini ni kwa mtizamo wa juu tu.

Kwani hata hivyo sisi Wafuasi wa (Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbali) tunadai kua hali halisi inatakiwa kuangaliwa kwa kutumia na mithili yake, kama wanavyosema kua Kubusu kunapelekea kuhitajia Udhu basi hakuna uthibitisho kutoka kwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum,* hususan pale inapokua uthibitisho unapingana na maamrisho ya Muumba mwenye kuamrisha.

Hivyo Imam Al Shawkani Al Hanbali anaendelea kusema kua: '**Bahr Al Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae *Allah Subhanah wa Ta'ala* Amemfundisha Tafsir ya Kitabu chake, kutokana na Kujibu Maombi ya Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam* ameweka wazi kua Kugusa kulikozungumziwa na Aya kunaashiria Kuingilian Kimwili.**

Na imedhihirishwa kua Tafsiri yake ndio Tafsir Bora zaidi kuliko Tafsiri za Wanazuoni wengineo, na hii inathibitishwa na kauli za Wanazuoni waliposema: Kinachomaanishwa ni kutokana na Kauli ya mmoja kati ya Mabedui alipomwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: "Mke wangu hakatai Mkono wa anaemgusa" - yaani akimaanisha kua ni Malaya.

Na ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Bedui huyo kua: 'Mpe Talaka.'

Hivyo baadhi wamesema kua Aya hii inazungumzia Kugusa Kumaanisha Kuingiliana Kimwili, nami sikuzungumzia juu ya hilo hapa kwa sababu sifikirii kua linatosheleza.

Ambapo kuhusiana na hadith basi haioneshi kua Udhu unabatilika, kwa sababu haijathibitishwa hali yake mhusika kabla ya *Rasul Alah Salallahu Alayhi wa Salam* kumuamrisha Kutia Udhu kama alikua tohara. Na haijathibitishwa kama alikua ana Udhu katika wakati alipomgusa Mwanamke husika, Na hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamwambia Kua Udhu wake umebatilika.'*(Nayl Al Awtar)*

Naam..huo ndio ufafanuzi wa Imam Ali Al Shawkani Al Hanbali katika kuelezea kuhusiana na Hukmu ya Madhhab ya Skuli ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Hanbal isemayo kua Kugusana na Jinsia nyengineyo hua hakutengui Udhu isipokua pale itakapokua kwa Matamanio. '**Kama ilivyosemwa katika Al Mughni na Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali Kua: 'Kugusa bila ya kua na Matamanio hakubatilishi Udhu kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akigusana na Mke wake, na Mkewe alikua akimgusa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pia, hivyo kama ingekua**

kunabatilisha Udhu basi asingemgusa. Na hakuna Tofauti juu ya kua kama Mwanamke huyo ni unaeweza kumuoa ama la, ni Mwanamke mzee au Kijana.'*(Al Mughni)*

Na amesema Imam Al Mardawi Al Hanbali kua: **'Miongoni mwa mambo yanayobatilisha Udhu basi Jambo la Tano ni Kugusana na Mwanamke kwa Matamanio, huu ndio Mtizamo wa Madhhab na ndio Mtizamo wa wengie miongoni mwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum*.'(***Al Insaaf)*

Na amesema Imam Abd Rahman Al Jazari katika Fiqh Alaa Madhdhahib Arbaa kua: '**Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wanasema kua: Udhu hubatilika kutokana na Kugusana na Mwanamke kwa Matamanio Bila ya kua na Kizuizi baina yao, iwe Mwanamke huyo ni Usiemjua akiwa katika Ihram, iwe ni mzima au amefariki, Mzee au Kijana au Mtoto.**

Na pia hali hii hua ni kwa Mwanammke atakapomgusa Mwanamme katika hali ya Matamanio. **Na Udhu hubatilika kwa kugusa pale itakapokua kulichoguswa si Nywele, wala Meno wala Kucha, kwani kugusa sehemu hizi hua hakubatilishi Udhu Ama kuhusiana na Mtu anaeeguswa kwa Matamanio basi Udhu wake hautobatilika hata kama atajisikia Raha, na haubatiliki kaa Mwanamme kumgusa Mwanamme hata kama atakua anavutia, na wala kwa Mwanamke kumgusa Mwanamke mwenzake, na Wala kwa Huntha kumgusa Huntha hata hama anaegusa atasikia raha.**

Na Udhu haubatiliki kwa kuangalia isipokua pale itakapokua kuangalia huko kutampelekea Anaeangalia Kutokwa na Kitu yaani Madhi*i.'**(Fiqh Ala Madhdhahib Arbaa)*

Naam..Alhamd lillah tumeangalia Mitizamo tofauti kuhusiana na Kubatilika na kutobatilila kwa Udhu kwa njia ya Lamas yaani kugusana baina ya Mtu wa Jinaia Moja na Jinsia Nyengine.

Na tumeona Mtizamo wa Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua Udhu hua haubatiliki kwa kugusana baina ya Mwanammke na Mwanamme isipokua pale tayari itakapokua Wanataka kuingiliana Ndio Utabatilika.

Na kwa tumeona kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kua wao wanasema kua Udhu Haubatiliki kwa kugusana baina ya Mwanammke na Mwanamme isipokua pale Mguso husika baina yao utakapokua ni wa Matamanio.

Na tumeona kua Ingawa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal wanafanana kimtizamo lakini pia kuna baadhi ya mambo wametofautiana juu ya hili.

Hivyo kabla kurudi katika Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi na tuangalie Mtizamo wa Imam Ibn Hazim Al Andalus katika kitabu chake cha Al Muhallah.

Ambapo Imam Abu Muhammad Ali Ibn Ahmad Ibn Said Ibn Hazim Al Andalus aliezaliwa mnamo mwaka 383 Al Hijr Mjini Qurtubi (Cordoba) Hispania na kufariki mwaka 447 Al Hijr alikua ni Muanzilishi wa Madhhab ya Dhahiri ambayo hayapo kwani yametoweka.

Hivyo anasema Imam Ibn Hazim Al Andalus kuhusiana yanayobatilisha Udhu kua**: 'Udhu Unabatilika kwa Mwanamme kumgusa Mwanammke na Mwanammke kumgusa Mwanamme, kwa kiungo chochote kile cha mwili ambacho mmoja wapo kati ya Watu wawili hawa atakitumia kwa kumgusa mwenzake.**

Iwe kwa Makusudi, Bila ya Kizuizi kama nguo au kitu chochote kile kitakachowatenganisha baina yao. Iwe Mtu husika amemgusa Mama yake au Binti yake, au Mama amemgusa Mtoto wake wa kiume au Baba yake, iwe ni Mtoto mdogo au ni Mtu Mzima hata kama hakuna matamanio katika Mguso husika.

Lakini kama wakigusana juu ya kizuizi kama Nguo basi Udhu huo hautotenguka, na hata kama ikiwa kuna Matamanio ikiwa wamegusana juu ya kizuizi basi Udhu hautotenguka. Na hivi ndivyo anavyosema Imam Al Shafii na wale wote wanaochukulia Mtizamo huu kutokana na maana ya moja kwa moja ya neno *Lamastumu An Nisaa* - Kugusana na Mwanamke.' *(Al Muhalla)*

Ambapo Imam Ibn Hazim anaelezea Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii huku akielezea Mtizamo wake yeye kwani yeye ni miongoni msa Wanaounga Mkono Mtizamo huu.

Na hivyo Imam Ibn Hazim anasema kua Hata kama ikiwa hakuna Matamanio baina ya watu wa Jinsia tofauti Wanaogusana basi Udhu wao Utabatilika, iwe wamegusana bila ya kizuizi kwa mikono, kwa vidole, nyuso, vifua, makalio, miguu n.k.

Lakini kama wakigusana juu ya kizuizi kama Nguo basi hata kama kuna hisia za Matamanio basi Udhu hautotengukwa kwa sababu kilichokisudiwa na maana ya aya ni kugusana ngozi kwa ngozi.

Hivyo tunaingia kwenye Mtizamo wa Wanazuoni wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu kutokana na Mtu Kugusana na Jinsia Nyengine.

Na hivyo kabla hatujaanza basi nadhani kwanza itakua vizuri tukiliangalia neno Lamasa ambalo ndio lililotumika katika Aya za Udhu na Tayammam kama tulivyoona hapo hapo kabla.

Kwani neno Lamasa kwa Kilugha hua liinamaanisha Kugusa,Kuhisi kwa Mkono, Kupapasa kwa Mkono, Kutafuta, Kuulizia na pia humaanisha Kuomba

Ambapo tunapoangalia Qur'an basi tunaona kua Neno Lamasa limetumika katika Aya za Udhu na Tayammam katika Surat An Nisaa 4:43 na Surat Al Maidah 5:6.

﴿أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدًا طَيِّبًا﴾

Aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban *(Surat An Nisaa 4:43, Surat Al Maidah 5:6).*

Tafsir: ***Au mnapo (لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi,***

Na kama tulivyoona katika aya hizi namna Wanazuoni walivyotofautiana juu yake kutokana na baadhi kutafsiri Moja kwa moja na baadhi kitafsiri kwa kumithilisha. Kwani baadhi wamemithilisha na Mfano wa Neno Masa lilotumika katika Aya ya Surat Al Imran 3:47 Pale Maryam Bint Imran alipohoji kwa kusema:

﴿قَالَتْ رَبِّ أَنَّىٰ يَكُونُ لِي وَلَدٌ وَلَمْ يَمْسَسْنِي بَشَرٌ﴾

Qalat Rabbi Anna Yakuunu Lii Waladu Walam yamsasnii Basharun. (*Surat Al Imran 3:47)*

Tafsir; ***Alisema (Maryam Bint Imran) Mola Wangu****: '****Nitawezaje Mimi kupata Mtoto Wakati Sijaguswa na Mtu'***

Hivyo mbali ya kua ni neno Lamasa lilotumika katika Aya mbili za Udhu na Tayammam zilizoanisha Sharti la:

﴿أَوْ لَـٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدًا طَيِّبًا﴾

Aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban *(Surat An Nisaa 4:43, Surat Al Maidah 5:6).*

Tafsir: ***Au mnapo (لَـٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi,***

Lakini pia limetumika katika aya zifuatazo ambazo zimemaanisha Kugusa kwa Mikono:-

﴿وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَاباً فِي قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ إِنْ هَـٰذَآ إِلاَّ سِحْرٌ مُّبِينٌ﴾

Walaw nazzaln<u>a</u> AAalayka kit<u>a</u>ban fee qir<u>ta</u>sin falamasoohu bi-aydeehim laq<u>a</u>la alla<u>dh</u>eena kafaroo in h<u>adha</u> ill<u>a</u> si<u>h</u>run mubeenun *(Surat Al Anaam 6:7)*

Tafsir: ***Na Hata Kama Tungekushushia Kitabu (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Katika Hali ya Karatasi Na Hivyo Wakakigusa kwa Mikono yao Basi Wangesema Wale wanaokufuru Huu si chochote isipokua ni Uchawi wa wazi.***

Na katika aya isemayo:

﴿وَأَنَّا لَمَسْنَا ٱلسَّمَآءَ فَوَجَدْنَاهَا مُلِئَتْ حَرَساً شَدِيداً وَشُهُباً﴾

Waann<u>a</u> lamasn<u>a</u> alssam<u>a</u>a fawajadn<u>a</u>h<u>a</u> muli-at <u>h</u>arasan shadeedan washuhub<u>a</u>n. *(Surat Al Jinn 72:8)*

Tafsir: ***(Wanasema Majini) Na Tulikua Tunajaribu Kugusa Mbingu Lakini Tukakuta Imejaa Walinzi Wakali wakiwa na Vijinga Vya Nyota Zimoto.***

Na pia neno Lamasa limetumika kumaanisha Kutafuta kama inavyosema Aya ifuatayo:

﴿يَوْمَ يَقُولُ ٱلْمُنَافِقُونَ وَٱلْمُنَافِقَاتُ لِلَّذِينَ آمَنُواْ ٱنظُرُونَا نَقْتَبِسْ مِن نُّورِكُمْ قِيلَ ٱرْجِعُواْ وَرَآءَكُمْ فَٱلْتَمِسُواْ نُوراً فَضُرِبَ بَيْنَهُم بِسُورٍ لَّهُ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ ٱلرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِن قِبَلِهِ ٱلْعَذَابُ﴾

Yawma yaqoolu almunafiqoona waalmunafiqatu lilladheena amanoo ondhuroona naqtabis min noorikum qeela irjiAAoo waraakum failtamisoo nooran fadhuriba baynahum bisoorin lahu babun batinuhu feehi alrrahmatu wadhahiruhu min qibalihi alAAadhabu*(Surat Al Hadid 57:13)***

Tafsir: ***Siku Hii Watasema Wanafik wa Kiume na Wanafik wa Kike Kuwaambia Wale walioamini Tusubirini ili Mtupatie Mwangaza kutoka kwenye Nuru zenu Wataambiwa Rudini Nyuma Mlikotoka Mkatafute Nuru! Hivyo Utapigwa Baina yao (Wanafiq na Waumini) Ukuta Wenye Geti Ndani yake Kutakua na Rehma Na Nje Yake Upande Unaokabiliana nao ukuta Huo kutakua na Adhabu.***

Subhanah Allah! Ama kuhusiana na aya hii ya mwisho basi imeshabadilisha Mada yetu kwa sababu inayoyazungumzia ni mazito na yenye kusikitisha sana yatakayowakuta Watu Wanafik katika Siku ya Malipo kabla ya kuvuka Daraja la Sirat.

Hivyo kwanza tumuombe *Allah Subhanah wa Ta'ala* atuepushe na Unafiq kwani Watakua ni wenye kupotea kwenye Kiza cha Unafiq wao huku wakiwa wanawaona Waumini wakiwa ni wenye kuokoka, baada ya kuwekwa ukuta baina yao na baada ya Wanafik kuambiwa kua Warudi nyuma walikotoka *Failtamisuu Nuuran - Wataiona Nuru* wanayoitafuta. Na hawatokutana na Nuru bali watakutana na Adhabu.

Na tunapoangalia maana ya Neno *Lamasa* ambalo humaanisha Kugusa, Kuhisi kwa Mikono, na Kutafuta. Na Ingawa neno *Lamas*a Hua linafanana na neno Massa mpaka Kimaana ila kuna tofauti baina ya Maneno mawili haya.

Kwani neno Massa hua linamaanisha Kugusa,Kutoa kitu kama kilivyo, Kupiga. Na pia kama Lilivyo neno Lamasa kua ni lenye kumaanisha Kutafuta, lakini Neno Massa humaanisha Kutafuta Kitu ambacho Hakiwezi kupatikana.

Na hivyo Neno Massa hua linamaanisha pia Kitu ambacho kinaeleza kujulikana hali yake kutokana na Mguso, na pia humaanisha Kuadhibu, Kudhuru na pia hua Linamaanisha Mguso wa Maingiliano ya Kimwili. Kama zilivyosema Aya zifuatazo baada ya *Bismi Allahi Rahmani Rahiim.*

﴿ وَإِن طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِن قَبْلِ أَن تَمَسُّوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيضَةً فَنِصْفُ مَا فَرَضْتُمْ إِلَّآ أَن يَعْفُونَ أَوْ يَعْفُوَاْ ٱلَّذِى بِيَدِهِۦ عُقْدَةُ ٱلنِّكَاحِ ۚ وَأَن تَعْفُوٓاْ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۚ وَلَا تَنسَوُاْ ٱلْفَضْلَ بَيْنَكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴾

Wa-in tallaqtumoohunna min qabli an tamassoohunna waqad faradtum lahunna fareedatan fanisfu ma faradtum illa an yaAAfoona aw yaAAfuwa alladhee biyadihi AAuqdatu alnnikahi waan taAAfoo aqrabu lilttaqwa wala tansawoo alfadhla baynakum inna Allaha bima taAAmaloona baseerun*(Surat Al Baqara 2:237)*

Tafsir: ***Na Kama ikiwa Mmewataliki (Wake zenu) Kabla Ya Kuwagusa (Kuwaingilia) Na Kama Mmeshakubaliana Mahari Basi Lipeni Nusu ya Mahari mliyokubaliana Ila Kama Atasamehe Mwanamke Au Atasamehe yule ambae Imo Mikononi mwake -Makubaliano ya Kufunga Ndoa (Mume) Lakini Kama (Mume) akimlipa Mahari yote basi huko hua ni Kukaribia Taqwa Wala Msisahau Fadhila Baina yenu Hakika Ya Allah Juu ya Mnayoyafanya anayaona.***

Na kama ilivyosema Aya nyengine kua:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا نَكَحْتُمُ ٱلْمُؤْمِنَٰتِ ثُمَّ طَلَّقْتُمُوهُنَّ مِن قَبْلِ أَن تَمَسُّوهُنَّ فَمَا لَكُمْ عَلَيْهِنَّ مِنْ عِدَّةٍ تَعْتَدُّونَهَا ۖ فَمَتِّعُوهُنَّ وَسَرِّحُوهُنَّ سَرَاحًا جَمِيلًا ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo idha nakahtumu almu/minati thumma tallaqtumoohunna min qabli an tamassoohunna fama lakum AAalayhinna min AAiddatin taAAtaddoonaha famattiAAoohunna wasarrihoohunna sarahan jameelan*(Surat Al Ahzab 33:49)*

Tafsir: ***Enyi wale ambao Mmeamini Mtakapowaoa Waumini wa Kike Na Kisha Mkawaacha Kabla Ya Kuwagusa (Kuwaingilia) Basi Itakua Hakuna Juu yao kuwahesabia Mda wa Kukaa Eda Kuhusiana Nao Basi Wazawadini (Wapeni Zawadi) Na Waachieni Huru Kwa Muachano Mzur****i.*

Na pia pale aya ziliposema:

﴿وَٱلَّذِينَ يُظَٰهِرُونَ مِن نِّسَآئِهِمْ ثُمَّ يَعُودُونَ لِمَا قَالُواْ فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مِّن قَبْلِ أَن يَتَمَآسَّا ۚ ذَٰلِكُمْ تُوعَظُونَ بِهِۦ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ﴾

Waallatheena yu*dha*hiroona min nisa-ihim thumma yaAAoodoona lima qaloo fatahreeru raqabatin min qabli an yatamassa dhalikum tooAAa*dh*oona bihi waAllahu bima taAAmaloona khabeerun*(Surat Al Mujaddila 58:3)*

Tafsir: ***Na Wale ambao Wanaojiharamishia (kwa kuwafanya Wake zao kua kama Mama Zao) Miongoni mwa Wake zao Na Kisha wakaataka Kujiachia Huru Juu ya Waliyoasema (ya Kuwaita Wake zao kua ni Mama zao) Basi (Kujisafisha Kwao Kafara yao) Ni Kuwacha Huru Mtumwa Kabla Hajagusana(Hajaingiliana) Nae Hilo ni Onyo kwenu(Ili msirudie Jambo hilo) Na Allah juu ya Mnayoyafanya Ni Mwenye Kua na Habari nayo***

Naam..hizo na Aya ya Maryam Bint Imran alipouliza Jee Nitapataje Mtoto Mimi wakati sijaguswa na Mtu? (SuratAl Imran 3:47) ni baadhi ya Aya zilizotumia pia asili ya neno Massa ambalo linafanana Kimatamshi na Kimaana na Neno Lamasa.

Na tumezianisha baadhi ili tusije tukajiuliza Masuali katika kufafanua kwetu, kwani kama tulivyosema kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wamemithilisha Kimaana neno Lamasa kua ni Kuingiliana Kimwili kama lilivyo neno Massa ambalo humaanisha Mguso wa Kuingiliana Kimwili.

Ambapo tunapoangalia Katika Kitabu cha Al Risala cha Imam Muad Idris Al Shafii Ambacho ndio kinachobeba Qawl Al Qadim yaani Kauli za zamani za Mitizamo ya Fiqh ya Imam Al Shafii basi tunaona kua anasema ndani yake Kua: '**Kugusana baina ya Mwanamme na Mwanamke hua hakutengui udhu isipokua kwa Matamanio.'** Ambapo huu ni Mtizmo unaofanana na Mtizamo wa Maimamu wa Madhhab mengineyo, kama tulivyoona hapo kabla.

Lakini tunapoangalia kitabu hiki cha Al Risala basi tunaona kua Imam Al Shafii alikiandika baina ya mwaka 195-198 Al Hijr yaani kabla hajahama kutoka Makkah kuelekea Misri. Na tunasema hivi kwa sababu Imam Muhammad Idris Al Shafii alikua ni Mtu wa kutafuta Ilm katika Maisha yake yote, Hivyo

Kila anaposikia kua Sehemu fulani iuna Mwanzuoni mwenye Ilm kubwa basi alikua ni mwenye kukimbilia kwa Mwanazuoni huyo ili anufike nae mbali ya kua yeye mwenyewe alikua ni tayari ni Imam mwenye Ilm Kubwa.

Hivyo mnamo mwaka 199 Al Hijra Imam Al Shafii alipata habari kua katika Ardhi ya Misri kuna Mwanazuoni aitwae Imam Al Layth Ibn Saad ambae ni mwenye Ilm kubwa kuliko Imam Malik. Hivyo Imam Al Shafii akakimbilia nchini Misri kwa ajili ya Kupata Ilm ya Imam Al Layth Ibn Saad lakini kabla ya Kufika Misri akapata Habari kua Imam Al Layth Ibn Saad ameshafariki Dunia. Na kwa kua nia yake ni kutafuta Ilm zaidi basi Imam Al Shafii hakuvunja Safari bali aliendelea na Safari kuelekea Misri kwa ajili ya kuipata Ilm ya Imam Al Layth Ibn Saad kupitia kwa Wanafunzi wake.

Na Hivyo Imam Al Shafii alippwasili katika Ardhi ya Nchini Misri basi akaanza kusoma kwa Wanafunzi hao huku na yeye akiwasomesha Wasiyoyajua kutoka kwake. Na Wakati Imam Al Shafii alipokua katika Ardhi ya Misri basi aliandika Kitabu kiitwacho Kitab Al Umm kabla ya kufariki kwake mnamo mwaka 204 Al Hijra.

Ambacho hiki Kitab Al Umm kama kinavyojitambulisha kwa Jina kua ni Kitabu Mama basi ndio kilikua kitabu Mama cha Mitizamo yake ya Fiqh kwani kilikua ni Kitabu chenye kubeba Mitizamo ya Zamani ya Fiqh na Mitizamo Mipya ya Fiqh katika masuali ambayo yaliyotofautiana katika Hukmu Zake.

Na kwa kua Al Umm ni Kitabu chenye Mitizamo Mipya yaani Al Qawl Al Jadid basi Imam Al Shafii alikikataa Kitabu chake cha Al Risala chenye Al Qawl Al Qadim yaani Kauli za Zamani ikiwemo kauli ya kuaKugusana na Wanawake hakubatilishi Udhu. Na hivyo akasema kua Atakaekifuata Kitabu Al Risala basi hana jukumu juu yake, maneno yenye kumaanisha kua Wafuasi wake wanatakiwa kutofuata Fatwa za zamani kwenye Al Risala bali wanatakiwa wafuate Mitizamo ya Kauli Mpya ya kwenye Kitab Al Umm.

Ambapo tunapoangalia sasa kwenye Kitab Al Umm kuhusiana na Kugusana na Jinsia nyengine basi tunaona anasema kua: ‘**Yeyote yule atakaegusana na Mwanammke kwa Mkono wake, bila ya Kuwepo kwa kizuizi baina ya Mkono wake na Mwili wake basi hua ni mwenye kuwajibikiwa n kutia Udhu.’***(Kitab Al Umm)*

Imam Muhammad Idris Al Shafii anaendelea kusema kua: **‘Iwe kugusana huko ni kudogo kwa mara moja tu, au kukubwa kwa mda, basi Udhu hua ni Wajibu**. **Iwe kwa Matamanio iwe La, basi Udhu ni Wajibu na hii ni kulingana na Hadith za Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* ambae amesema kua: Yeyote atakemgusa Mke wake kwa mkono au kum-busu hivyo yeyote atakaemgusa au kumbusu Mkewe basi Udhu unamuwajibikia.’**

Na Abd Allah Ibn Masud Ra*dhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: Mtu anatakiwa kutia Udhu baada ya kugusana moja kwa moja kwa mkono na baada ya kubusiana na mkewe. **Na hii pia ni kutokana na Maneno ya Waziwazi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema: Aw Lamastumu Al Nisaa - Au Mtakapogusana na Wanawake, ambapo haikusemwa kama kwa Matamanio ama La**.’*(Kitab Al Umm)*

Ila hapa sasa nataka turudi Nyuma kidoogo kwani inabidi tufahamishane kuhusiana na Mtizamo huu, kwa sababu kama hatukufahamiana basi tutachanganyana tena sana. Hivyo kwanza huu ni Mtizamo wa Imam Muhammad Idris Al Shafii lakini huu si Mtizamo unaokubalika katika Skuli ya Madhhab ya Imam Al Shafii

Na hii ni kwa sababu Mtizamo wa Kila Skuli ya Madhab hua hautegemeani na Imam Mkuu wa Madhhab peke yake bali hua unategemeana na Makubaliano ya Maimamu Wakuu wa Fiqh wa Madhhab Husika katika Jambo husika

Na maana baadhi ya Wakati tunakua tunasema kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kwa mfano kuhusiana na jambo fulani kua Imam Abu Hanifa juu ya Jambo hili amesema hivi, lakini kwa upande wa Imam Abu Yusuf basi ambae yeye ni Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa basi amesema hivi, au kwa Upande wa Imam Muhammad Ash Shaybani ambae ni Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa basi yeye amepingana na Imam Abu Hanifa juu ya hili kwa kusema hivi, n.k.

Na tukisema Imam Al Sarkhasi Al Hanafi au Imam Al Muhaqqiq Ibn Aabidin Ash Shami Al Hanafi basi yeye amesema kua Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa juu ya Hili ni kadha wa kadha. Basi huu ndio Utakua Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, na hii ni kwa Sababu Imam Ibn Aabidin kutokana na kua na Sifa ya kua ni Al Muhaqqiq yaani Mhakikishaji wa Kauli za Maimamu wote wa kabla yake wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa juu ya jambo husika na baada kuhakikisha Kulingana na vithibitisho na Mitizamo ya Maimamu wa Fiqh ya Imam Abu Hanifa basi Imam Ibn Aabidin au Imam Al Sarkhasi hua ni mwenye kuhitimisha kua kuhusiana na Jambo hili basi Maimamu wengi wamekubaliana na Mtizamo wa Imam Abu Hanifa, basi Fatwa yake ni Mtizamo huu.

Na hivyo kama ikiwa Maimamu wengi wamepingana na Imam Abu Hanifa lakini wakawaunga Mkono Wanafunzi wa Imam Abu Hanifa, mmoja kati ya Wanafunzi wake basi Mtizamo wa Madhhab ya Hanafi utakua Katika Jambo husika utakua ni Kulingana na Mtizamo wa Wanafunzi wa Imam Abu Hanifa.

Sasa tunarudi kwenye Madhhab ya Imam Al Shafii ambapo kama tulivyoona kuhusiana na Mtizamo wa Imam Al Shafii, lakini tukiangalia Mtizamo wa Imam Abu Is-haq Al Shirazi basi yeye amesema kua kuna Mitizamo zaidi ya miwili juu yake na akafafanua kama tulivyoona na kisha akasema Mtizamo Sahih ni kua Mtu asieweza kuoana nae basi hakitengui Udhu. Ambapo Imam Abu Is-haq Al Shirazi aliishi Miaka 250 baada ya Kufariki Imam Al Shafii.

Kwa maana hio basi baina ya Imam Al Shafii na Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii kuna Wanazuoni Wakuu kadhaa wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii wakiwemo:

Imam Is-haq Ibn Rahawayh Al Shafii.
Imam Al Muzani Al Shafii.
Imam Al Buwayti Al Shafii.
Imam Abu Thawyr Al Shafii.
Imam Al Rabbi Ibn Sulayman Al Shafii.
Imam Al Zafarani Al Shafii.
Imam Al Darimi Al Shafii.
Imam Ibn Al Mundhiri Al Shafii.
Imam Al Anmati Al Shafii.
Imam Ibn Surayj Al Shafii.
Imam Abu Is-haq Al Marwazi Al Shafii.
Imam Abu Zayd Al Marwazi Al Shafii.
Imam Abu Qasim Al Dariki Al Shafii.
Imam Abu Hamid Al Isfarrayini Al Shafii.
Imam Abu Tayyib Al Tabari Al Shafii.
Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii.

Naam..Hivyo baina ya Imam Al Shafii na Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii kuna Maimamu 15, na hivyo juu ya jambo hili kuna Mitizamo ya Maimamu Wakuu 17 wa Fiqh wa Madhhab ya Imam Al Shafii katika wakati wa Uhai wa Imam Abu Is-haq Al Shirazi.

Kwa Maana hio basi Imam Abu Is-haq ameipitia Mitizamo ya Maimamu 15 wa Madhhab ya Imam Al Shafii na vithibitisho vyao na kisha akaangalia Makubaliano yao juu ya Kutenguka kwa Udhu baada ya kugusana na Jinsia nyengine na kisha ndio akahitimisha alivyohitimisha.

Ambapo hata hivyo kaa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Fatwa ya Madhhab inapatikana kutoka kwa Wahitimishaji Wakuu ambao ni Imam Al Rafii, Imam An Nawawi, Imam Ibn Hajar Al Haytami na Imam Al Ramli ambao wote hawa walifuatia hapo baadae.

Na hivyo ili kupata Mtizamo Unaokubalika wa Madhhab basi inabidi tuangalie Makubaliano ya Wanazuoni wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kutoka katika Hitimisho la Maimamu hawa Wanne juu ya Mtizamo wa Imam Al Shafii na Maimamu wengine wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu kutokana na Mtu Kugusana na Jinsia Nyengine. '**Kwani kama tulivyoona kua katika Qawl Al Qadim, Imam Al Shafii amesema kua hakutengui Udhu na katika Qawl Al Jadid amesema kua Kunatengua iwe Mwanamke huyo ni Mahram au Ajnabi kwako na kwa Mwanamke pia unatenguka we ni Mahram kwake au Ni Ajnabi kwake.**'

Lakini kabla ya kuendelea basi bora tufafanue Neno Ajnabi Maana yake ni nini?
Na tunapoangalia maana basi tunaona kua Neno Ajnabi linatokana na neno Janaba ambalo tulifafanua hapo kabla katika kufafahamishana kuhusiana na Hukmu za Janaba ambapo tulisema kua Neno Janaba hua linamaanisha Kugeuka, Kutenga Kuweka Upande, Kuweka Mbali, Kukataa Kitu, Kua mbali na Kitu.

Neno Janaba ndio lililotoa neno Junub ambalo huumaanisha Mtu Mgeni, Mtu wa Mbali, na pia humaanisha Mtu ambae anatakiwa Kujitoharisha kwa kukoga

Neno Janabah limetoa pia neno Ajnabi ambalo humaanisha Mtu ambae ni wa Mbali nawe Kidamu na Hivyo Unaruhusika Kuoana nae.

Kama anavyosema Imam Muhammad Al Zuhayli Al Dimashq Al Shafii kua: **'Mwanamke Ajnabi hua ni Mwanamke ambae Mtu anaruhusika Kuoana nae, na Mahram hua inamaanisha Mwanamke ambae hairuhusiki na ni Haram kuoana nae.'***(Al Mutammad Fi Fiqh Al Shafii)*

Hivyo tunaporudi katika Mada yetu basi tunaona kua Imam Abu Is-haq Al Shirazi alitoa Mitizamo kadhaa tofauti juu ya Kubatilikana kutobatilika kwa Udhu katika Kitabu chake cha Al Muhadhdhab ukiwemo Mtizamo wa Imam Al Shafii tulioangalia hapo kabla Na tukasema kua ili kupata Mtizamo unaotegemewa na unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii juu ya Mada hii basi inabidi tuangalie Mitizamo ya Maimamu Wakuu wa kuhakiki Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ni Imam Al Rafii, Imam An Nawawi, Imam Al Ramli na Imam Ibn Hajar Al Haytami

Hivyo tunatua kwa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi katika kitanu chake cha Al Majmju Fii Sharh Al Muhadhdhab ambacho ni Ufafanuzi wa Kitabu cha Imam Abu Is-haq Al Shirazi cha Al Muhadhdhab. Ambapo ndani yake tunaona kua Imam An Nawawi anasema kua: '**Kwa Hakika Mgusano baina ya Mwanamme na Mwanammke ambao ni Ajnabi hua ni Moja kati ya Mambo ambayo Yanabatilisha Udhu, iwe kwa kutamaniana ama la. Ila kama ikiwa Mgusano huo umetokea huku kukiwa na Kizuizi baina yao hata kizuizi hicho kikiwa ki chepesi basi Udhu hautobatilika.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Ambapo Imam Muhammad Al Zuhayli Ad Dimashq Al Shafii ambae ni Mwanafiqh Mahiri wa Karne yetu akathibitisha zaidi Mtizamo huo katika Kitabu chake cha Mitizamo Inayokubalika na Kutegemewa zaid katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kitwacho Al Mutammad Fi Fiqh Al Shafii kua: **'Kugusana na Mtoto mdogo wa Kike Ajnabi hua hakubatilishi Udhu kama ikiwa hakuna Matamanio ndani yake, na pia kugusa Nywele, Kucha na Meno ya Ajnabi hakitengui Udhu, ila kugusana na Ajnabi Mzee hua kunabatilisha Udhu iwe kugusan huko kunatokana na Matamanio ama la.'***(Al Mutammad Fi Fiqh Al Shafii)*

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Kama zikigusana Ngozi ya Mwanamme na Mwanamke Ajnabi basi Udhu wa Aliegusa Utatenguka iwe aliegusa ni Mwanamme au ni Mwanammke Iwe mguso huo ulikua ni wa Matamanio ama la, iwe baada ya mguso huo kumetokea raha ya Matamanio ama la; iwe Mguso huo ni wa Makusudi au wa Kutokusudia iwe kwa kukosea au kwa kutokea kwa bahati mbaya.**

Iwe mguso huo ni wa mda mfupi au ni wa mda mrefu au ni wenye kukatishwa hapo hapo kwa haraka sana mara tu baada ya kugusana Iwe mguso huo umetokana na sehemu ya kiungo kinachotakiwa kutiwa Maji katika Wakati wa kutia Udhu ama la, iwe mguso huo ni kwa ajili ya mtu aliepooza na hivyo kutokua na hisia katika sehemu husika ama la, iwe kiungo kilichozidi katika mwili ama la.

Kwani mguso wa hali zote hizo hua ni wenye kutengua Udhu kwa Upande wa Skuli yetu ya Madhhab ya Imam Al Shafii Na huu ndio pia Mtizamo wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* Zayd Ibn Aslam *Radhi Allahu Anhu.*

Na ndio Mtizamo wa Imam Makhul, Imam Ataa, Imam Ibn Al Saib, Imam Al Zuhri, Imam Yahya Ibn Said Al Ansari, Imam Rabia, na Imam Said Ibn Abd Al Azizi na pia ndio mtizamo mmoja kati ya Mitizamo miwili ya Imam Al Awzai.'(*Al Majmuu Fii Sharh Al Muhadhdhab)*

Na amesema Imam Sulayman Al Bujaraimi Al Shafii kua: **'Fahamuni kua Mguso hubatilisha Udhu kutokana na Moja kati ya Hali Tano zifuatazo:**

1-Hali ya kua Waliogusana ni watu wa Jinsia Tofauti, yaani Mwanamme na Mwanamke.

2-Mguso huo uwe ni wenye kupitia kwenye Ngozi yaani isiwe kwenye Nywele au Kucha au Meno.

3-Mguso huo Uwe ni Mguso wa moja kwa Moja Ngozi kwa Ngozi bila ya kua na Kizuizi baina yake.

4-Mguso huo uwe kwa watu ambao wako katika Umri wa kuweza kua na Matamanio.

5-Mguso huo uwe ni Baina ya Watu ambao ni Ajnabi na hivyo Wasiwe Mahram.'*(Hashiyah Al Bujaraimi)*

Ambapo Mtizamo huu wa Imam Sulayman Al Bujaraimi umefafanuliwa tena na Imam Muhammad An Nawawi Ibn Umar Al Jawi Al Shafii katika Kitabu chake cha *Kashif Al Saja Fi Sharh Safinat Al Najah.*

Na amesema Imam Habib Ibn Ahmad Ibn Muhammad Ibn Salim Al Kafi Al Madani Al Shafii kua: **'Kulingana na Mtizamo Unaokubalika na Unaotegemewa zaid katika Skuli ya Madhhab ya Imam**

Al Shafii juu ya Mgusano wa Ngozi baina ya Mke na Mume basi ni kua Hua kunabatilisha Udhu iwe kwa Matamanio ama la, kwani hawa hua ni Ajnabi.'*(Taqrirat Al Sadidah Fi Masail Al Mufidah)*

Na Imam Abu Jaffar Muhammad Ibn Jarir Ibn Yazid At Tabari Al Shafii kua: **Amesema Nafii Mawla Ibn Umar kua: Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alikua Akitia Udhu baada ya Kubusiana na Mke wake na alipoulizwa kwanini basi alisema: Ni Kutokana na Mguso'**

Na Imam Abu Muhammad Abd Rahman Ibn Abi Hatim Al Tamimi Al Hanzala Al Shafii amesema kua Wengi miongoni mwa Tabiina wamenukuu juu habari hii na walikua wakisema kua: '**Kinachopelekea Kutia Udhu ni maana ya Wazi ya Neno Lamastu katika aya isemayo:**

﴿وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَاباً فِي قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ إِنْ هَٰذَآ إِلاَّ سِحْرٌ مُّبِينٌ﴾

Walaw nazzalna AAalayka kitaban fee qirtasin falamasoohu bi-aydeehim laqala alladheena kafaroo in hadha illa sihrun mubeenun *(Surat Al Anaam 6:7)*

Tafsir: ***Na Hata Kama Tungekushushia Kitabu(Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Katika Hali ya Karatasi Na Hivyo Wakakigusa kwa Mikono yao Basi Wangesema Wale wanaokufuru Huu si chochote isipokua ni Uchawi wa wazi.***

Imam Ibn Abi Hatim anaendelea kusema pia **na pia ni kutokana na Neno Lamas katika Hadith ya Abd Allah Ibn Ababs *Radhi Allahu Anhu* isemayo: Maiz Ibn Malik Alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomuuliza Maiz Ibn Malik baada ya Kukiri kufanya Kitendo cha Aibu na Mwanamke asiekua Mke wake na hivyo anaomba Aadhibiwe**

أنَّ ماعزَ بنَ مالكَ أتَى النَّبيَّ صلَّى اللَّهُ عليهِ وسلَّمَ ، فقالَ لَهُ : لعلكَ قبَّلتَ أو لَمستَ أو غَمزتَ

. قالَ لا

. قالَ :فعلتُ كَذا وكَذا ؟ لا يُكنِّي

. قالَ : نعم

فأمرَ برجمِهِ

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Maiz kwa kusema: 'Jee umembusu? Umemgusa? Au Umemkonyeza?'

Na hivyo Maiz akasema: 'La.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Umeingiliana nae?'**

Maiz akasema 'Naam'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamrisha kua Maiz apigwe Mawe.*(Al Iqtirah fi Bayan Al Istilah-Imam Ibn Daqiq Al Eid, Imam At Tabarani, Imam Al Bukhari na Muslim)*

Imam Ibn Abi Hatim anaendelea kusema kua na pia Kutokana na Hadith iliyotumia neno Lamasa isemayo kua**:**

" أن رسول الله صلى الله عليه وسلم نهى عن بيع الملامسة

‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza Kununua Kitu kwa Kugusa tu’

Ambapo Kuuza na kununua kwa Kugusa tu Bidhaa kuliko katazwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kulingana na Mtizamo wa Fiqh kunazungumziwa hapa hua kunamaanisha Kua Mnunuzi hatakiwi kununua Bidhaa kwa kutegemea Mguso wa nje tu wa bidhaa hio bila ya kuiangalia na kuichunguza vizuri na hivyo kutopata kujua uhalisia wake kama itamfaa bidhaa hio ama la, Nzima ama mbovu n.k.

Hivyo katazo la *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Hadith hii ni kutodhulumiana bali kufanyiana Uadilifu katika biashara.

.

Imam Ibn Abi Hatimm anaendelea kusema kua Na pia neno Lamas katika Hadith isemayo kua ‘**Na uzinifu wa Mkono ni katika Kugusa.’**

Na pia katika Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* isemayo kua: ‘**Hakukua na Siku isipokua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akitupitia Wake zake na Kutugusagusa na Kutubusubusu**.

Ambapo Vithibitisho vyote hivi vinathibitisha kua neno Lamastum ni Kugusa kwa Mkono*(Al Mawsuat Alshamilat Liltafasir)*

Na anasema Shaykh ul Islami, Imam Al Muhaqqiqiin Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Ansari Al Shafii kua:

Jambo la Tatu linalobatilisha Udhu ni Kugusana kwa Ngozi, ambapo kwa upande wa Mwanamme basi hua ni Mwanamme *ajnabi* Mwenye Kutamanika Kimaumbile Na bila ya Shaka hii hua ni kwa Wale wenye Akili Timamu iwe ni Mtoto au Mtu Mzima.

Kwa Mwanamke basi ni Mwanamke *ajnabi* mwenye Kutamanika kimaumbile na bila ya shaka kwa wale wenye akili timamu iwe mtoto au Mtu Mzima.

Hivyo hata kama itakua mmoja wao miongoni mwao baina ya Watu wawili hao Mwanamme na Mwanamke atakua ameguswa kwa nguvu basi Udhu wao Utawatoka. Ila kama itakua Mmoja wao ni Maiti basi Bila ya Shaka Udhu wa Maiti hautobatilika

Na kuna Baadhi wamesema kua Hata Kugusana na Jini wa Jinsia Nyengine basi Udhu Utabatilika, ila bila ya Shaka hii itakua Sahih kama Ikiwa Inaruhusika kuoana nao Majini, lakini hairuhusiki

Na hii ya kubatilishika kwa Udhu baina ya Jinsia Tofauti ni kutokana na Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala yasemayo*:

﴿أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ﴾

Aw Lamastumu Al Nisaa - Au Mkigusana na Wanawake.

Aya ambayo ni yenye kumaanisha Kinyume na Hadith isemayo kua: Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alikua akiwabusi wake zake na kisha husali bila ya Kutia Udhu" - Ambapo hii ni Hadith Dhaif katika sehemu mbili za Mnyororo wa Nukuu yake

Ama kuhusiana na Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* ambayo inasema kua alikua akigusana na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* wakati alipokua Akisali Basi hii Hadith inaelezea hali ambayo inawezekana ikawa alikua akimgusa kwa baina ya Kizuizi.

Kwani kugusa kwa kawaida kwa Mkono hubatilisha Udhu, na hii ni kwa sababu kugusa hua chanzo cha Matamanio hivyo hua ni kwenye kuamsha hisia za Matamanio, jambo ambalo hua silo kaa Mtu mwenye Kua na Tohara.

Na kipimo chake Mguso husika hua ni kutokana na Kua ni Mguso wa Mtu tofauti kumgusa mwengine, iwe mguso huo ni wa Mtu alipooza Mwili Au hana Matamanio na hata kama ikiwa ni kwa mda mfupi tu na hususan Mguso huo ukiwa unatokana na Kiganja cha Mkono.

Na Mguso wa ngozi iliyokusudiwa ni sehemu ya Nje ya Mwili na hivyo ndani yake hua pia mnajumuishika hata Ufizi na Ulimi.

Lakini sehemu ya Ndani ya Jicho haijumuishiki tofauti na alivyosema Imam Ibn Ajil, na hii ni kwa sababu sehemu ya Ndani ya Jicho chini ya Kope na Mboni yake hua si sehemu yenye kupokea Hisia za Raha inapoguswa.

Ambapo Mboni na chini ya Kope hua ni tofauti na Ufizi na Ulimi, hivi jee huoni kua Ulimi wa Mke hua unastarehesha kwa kunyonywa na kuguswa?'

Kama ilivyothibitishwa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Ulimi wa *Aisha Radhi Allahu Anha.*

Na hivyo hua ni tofauti na sehemu za ndani ya Jicho, na tofauti na wale wanaosema kua sehemu ya ndani ya Jicho atarehe yake ni katika Kutizama kunakopelekea Mtu kutaka Kugusa, jambo ambalo halihusiani Na Mguso, ama kuhusiana na Meno na Nywele na Kucha basi ni kua vitu hivi huota, huchomoza na kisha hutoweka, hivyo hamna uthibitisho ndani yake kihisia.

Isipokua raha yake ni katika kuvitizama vitu hivyo bila ya kuvigusa,na hivi ndivyo pia hali ilivyo kwa sehemu ya ndani ya Jicho.

Na bila ya shaka hua hakuna Tofauti baina ya Mgusaji na alieguswa katika kubatilishika kwa Udhu wao kwa sababu wote hua na Uwezekano wa kuamshika kwa hisia zamatamanio yao, kama vile ambavyo inavyokua kwa Wanaoingiliana kimwili.' *(Tuhfah Al Muhtaj bi Sharh Al Minhaj)*

Na anasema Shaykh ul Islami, Shams Ad Din Muhammad Ibn Abi Al Abbas Ahmad Ibn Hamza Shihab Ad Din Al Ramli Al Shafii katika Nihayat Al Muhtaj aAla Sharh Al Minhaj kua: '**Jambo la Tatu linalobatilisha Udhu ni Kukutana kwa Ngozi ya Mwanamme na Mwanamke, hata kama si kwa Matamanio, hata kama ikiwa ni kwa Mghafiliko au kusahau.**

Na Maana yake ni kua Ngozi ni kiungo cha Hisia kinachoamsha Matamanio, iwe kwa Mwanamme Kijana Shababi, kwa asiekua na Nguvu za Kiume, kwa aliehasiwa, au aliepakwa mafuta, iwe kwa Mwanamme au kwa Mwanammke.

Iwe kwa Mtu mzima asietamaniwa, asiekua na Matamanio, kwa sababu kika kitu kinachodondoka basi hua kina Muokotaji wake iwe kwa kuguswa kwa Mikono au kwa kitu chengine Iwe sehemu ya Ngozi hio ni ya kiungo cha ziada tofauti na maumbile, iwe ni kiungo chenye Afya au kilichopooza.

Na hii ni kutokana na Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo kua:

﴿أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ﴾

Aw Lamastumu Al Nisaa - Au Mkigusana na Wanawake*(Surat Al Maida aya ya 6)*

Maneno ambayo yanamaanisha kua Mkigusana kama yanavyosomeka na kugusa hua kunatokana na Mikono. Na pia kama alivyofafanua Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema kua Si Kwa kuingiliana Kimwili Kwa sababu kuingiliana hua ni Kinyume na Maana iliyowazi, na pia Lamastumu - Kugusana kulikotajwa hapa katika Aya kumejumuishwa na Kutoka Chooni na amrisho la Kufanya Tayammam kama ikiwa hakuna Maji.

Na hivyo Hii Kugusana Ngozi baina ya Mwanamme na Maanammke ajnabi hua kunajumuishwa kua ni kama kua na Najis kama vile mtu atokae Chooni. Hivyo kinachobatilisha Udhu hua ni Ngozi na wala si Nywele, wala Meno wala Kucha. **Na Ndani yake inajumuishika Mfupa wa Ndani ya Mwili kama ukiyokeza nje na ukaguswa na Ajnabi basi Udhu Hubatilika.'***(Nihayat Al Muhtaj Ila Sharh Al Minhaj -Imam Al Ramli)*

Ama kuhusiana na Mafuta basi Kuna aina ya Mafuta mbali mbali kama ya Misk, Haba Soda, Zaytun, Sandalwood, na hata Marashi n.k ambayo hua yanasomewa kisha Mtu anajipaka na hivyo kutokana nayo hua anapata utulivu wa kimwili, kiakili na kiroho kulingana na Mafuta na kisomo husika, na pia kulingana na harufu ya Mafuta husika kwa mfano Harufu nzuri ya mafuta inaashiria uwepo wa baraka na ulinzi wa dhidi ya Ibilisi, na hivyo kumfanya mtu kuingia kwenye hali ya unyenyekevu na Ikhlasi kiibada hivyo baadhi ya mafuta hua yanaweza kumuondolea mtu Matamanio na kukuweka mbali na vishawishi vya Ibilisi.

Ambapo Imam Abu Al Diya Nur Ad Din Ibn Ali Al Shabramilisi Al Aqhari Al Shafii anasema katika Hashiyah Al Shabramilisi kua: '**Mgusano wa baina ya Ngozi ya Ajnabi wa Jinsia ya Kiume na ya Kike kunajumuisha na Viumbe Majini pia. Na hii hujumuishika pale itakapokua Mwanamme ameguswa na Jini ambae imethibitishika kua ni Jike.**

Kama vili ilivyokua kuna Mtizamo wa kuruhusika Kuoana baina ya Jini na Ibn Adam, ambao ni Mtizamo tofauti na Mtizamo wa Wanzuoni wengine. **Ambako hua kunatofautiana na kua na shaka juu ya jinsia ya alieguswa, kwani Shaka hua haibatilishi ndoa Ila Suali hua linakua Jee Jini Husika ni Jike au Dume lililojigeuza kua ni Jike?, na Jee Ndoa husika Itabatilika ama la?'**

Ambapo Jibu lake nisemalo mimi ni kua Maana halisi hua ni kutegemeana na uhalisia wa Awali na hivyo hakuna kitakachobatilika. **Na hii ni kutokana na uyakini wa kua Mtizamo wa Jicho haukubadilika bali kilichobadilika ni Maumbile ya Jini kutoka katika haki moja kuingia katika hali nyengine huku asili yake ikiwa imebakia ile ile Ya Awali.**

Ama kuhusiana na Mabadiliko ya Muonekano wa Jini husika basi Huweza kubatilisha Udhu kutokana na kubadilika kwa muonekano wa Mtizamo wa Jicho, ambapo hata hivyo tunaweza

kusema kua Udhu hautobatilika kwa sababu Jini anaweza kujibadilisha bila Kugundulika kwa Mtizamo wa Jicho.'*(Hashiyah Al Shabramilisi)*

Imam Shabramilisi anaendelea kutuambia kua: '**Ama kuhusiana na kauli ya Imam Isemayo kua:Kila kinachodondoka hua kina muokotaji wake Basi ni yenye kumaanisha kua Hakuna Tunda linaloanguka kisha likakosekana kuonekana na Mtizamo wa Watu kutokana na Kua chini kwake au kutokana na Harufu nzuri yake ambayo humpelekea Mtu kuliokota.**

Hivyo kwa upande wa Mwanammke hata kama akiwa mzee na mbaya vipi basi lazima kutakua na Mwanamme anaemtamani Mwanammke huyo kwa Moyo wake na Roho yake.' *(Hashiyah Shabramilisi)*

Na Alhamd lillah tunaona kua kila tunavyozidi kuangalia Mitizamo ya Maimamu tofauti wa Madhhab ya Imam Al Shafii juu ya Jambo hili basi ndio Tunavyozidi kupata ufafanuzi zaidi.na kupata manufaa zaidi. Hivyo na tunaangalia Mtizamo wa Mwanafunzi wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii ambae ni Mwalimu wa Imam Ahmad Al Qastallani Al Shafii na pia Mwalimu wa Al Muhaqqiq Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Maki Al Shafii na Maimamu wengineo.

Na huyu si mwengine isipokua ni Shaykh Ul Islami Al Allama Imam Zayn Ad Din Al Sunayki Abu Yahya Ibn Muhammad Ibn Zakarriyah Al Ansari Al Shafii: '**Na Jambo la Tatu linalotengua Udhu ni Kugusana kwa Ngozi baina ya Mwanamme kwa Mwanamke na Mwanamke kwa Mwanamme. Na hii ni kutokana na Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala pale* aliposema katika Qur'an kua**

﴿أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ﴾

Aw Lamastumu Al Nisaa - Au Mkigusana na Wanawake(*Surat Al Maida aya ya 6)*

Ambako kunamaanisha Kugusana kama inavyosomwa aya na wala haimaanishi Kuingiliana Kwa Sababu Kuingiliana hua si Kugusana kwa Mikono, wala si kwa Mkono na wala si kugusana bila ya Mikono, kama alivyosema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*

Na maana ya kutofautiana kwake hua ni kutokana na kua Kugusana hua ni kwenye kupelekea kutokea hisia za Raha ya Matamanio kwa Ajnabi yaani anaeweza kuoana nae Mtu ambayo hukosekana pale inapokua ni kugusana kwa Mahram wake kutokana kutoruhusika kuoana nae mtu Iwe kutokana na Udugu ukaribu wa Damu, wa Unyonyaji wa ziwa Moja au wa Ndoa.

Ama kuhusiana na Kugusana huko basi hua ni kwa Ngozi tu na wala hakui kwa Nywele, Meno au Kucha. Hivyo Hata kama Ngozi ya Mtu itakua Imejaa Vumbi tuseme lililogandana na Ngozi kutokana na Jasho basi Udhu utabatilika kwa sababu Vumbi hilo limeshikamana na Ngozi na kua kama Ngozi yenyewe.

Na kuhusiana na Umri wa Mtoto mdogo asietengua Udhu basi hua ni kulingana na Utamaduni wa Jamii husika kumaanisha kua Katika Umri husika basi Mtoto hua Hatamaniwi na hivyo hii hua ni kuanzia Miaka Saba kushuka Chini.

Hivyo Mtoto Ajnabi akizidi Umri wa Miaka 7 hua anatenguka Udhu akiguswa na hua anatengua Udhu wa aliemgusa na hii ni kwa sababu katika Umri huo mtoto hua anahisi hisia za Raha kama anazohizi anaemgusa.

Na Udhu unatenguka kwa kugusana na Maiti wa Kike kwa Mwaname, wa Kiume kwa Mwanamke, na kwa Kizee na kiungo kilichopooza Na hii bila kuangalia kama Kugusa huko ni kwa Makusudi, kwa bahati mbaya, kwa Matamanio au bila ya Matamanio na hata kama ikiwa kugusana huko si kwa Mkono.

Ama kuhusiana na Kugusa Nywele, Kucha au Meno basi hakutengui kwa sababu hua hakuna raha ya Matamanio katika kugusa kwake, bali Matamanio hutokea kwa kuona na anaegusa vitu hivyo hua hakugusa Mtu Mwanamme wala Mwanamke.

Na Wala hakubatilishi Udhu muonekano wa Ajnabi ambae ni Mzuri sana Kwa Kumtizama kwa Macho wala Kumkaribia karibu nae bila ya kumgusa, kwa sababu hilo halikujumuishwa kwenye Aya.

Na aya inadhihirisha kua kutowezekana kubatilika kwa Udhu kwa kugusana kwa ngozi baina ya Wanaume kwa Wanaume, Wanawake kwa Wanawake au Huntha Wawili au Huntha na Mwanamme au na Mwanammke,hata kama ikiwa ni kwa Matamanio, na hii ni kwa sababu asili yao kimaumbile migusano ya Wanaume kwa Wanaume, Wanawake kwa Wanawake n.k hua ni Tohara.'*(Asna Matalib Sharh Rawdh At Talib-Ima Zakarriyah Al Ansari)*

MUBTILAT SALAT - KUGUSANA NA JINSIA NYENGINE KATIKA IBADA YA HIJA

❖❖❖❖

Kama tulivyoona kua kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Udhu hua ni wenye kubatilika pale inapotokea Mgusano wa Ngozi baina ya Mwanamme na Mwanamke wanaoruhusika Kuoana, iwe kugusana huko ni kwa Makusudi Ama la, kwa Matamanio ama La.

Ambapo hili hua ni Jambo linalochanganya Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii Pale tunapozungumzia kuhusiana na Ibada ya Hija hususan katika wakati wa Tawwaf yaani Kuzunguka Al Kaabah kutokana na kutowezekana kwa Mtu Kujichunga ili asigusane na Ajnabi yaani na Mtu wa Jinsia nyengie ambae anaeweza kuoana nae, kutokana na Msongamano wa Wingi wa Watu katika Kuzunguka Al Kaabah.

Ambapo vithubitisho vya Sharia vinathibitisha kua Mtu yeyote yul asiekua Tohara basi hua ni mwenye kitakiwa kujitoharisha kabla ya Kuingia kwenye Ibada Ibada ya Tawwaf ya Hijja au Umra, Kusoma Qur'an na kila Ibada inahitajia kua Tohara ili ikubalike mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*.

Na kuhusiana na Tawwaf basi amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua**:**

أن النبي صلى الله عليه وسلم أول شيء بدأ به حين قدم مكة أن توضأ وطاف بالبيت

Alikua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Jambo la Kwanza alilofanya alipowasili katika Mji wa Makkah ni kua alitia Udhu na kisha Akazunguka Al Kaabah.'*(Sahih Bukari na Muslim)*

Na bila ya shaka Hakuna Ibada ya Umra wala Ibada ya Hija bila kufanya Tawwaf, kwani amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kumwambia Aisha *Radhi Allahu Anha* ambae alilalamika kua ameingia kwenye Siku zake wakati walipowasili Katika Mji wa Makkah, kwa ajili ya Ibada ya Hija kua:

: افْعَلِي كما يَفْعَلُ الحَاجُّ غيرَ أَنْ لا تَطُوفِي بالبَيْتِ حتَّى تَطْهُرِي

‘Fanya kama wafanyavyo Mahujaji ila Usifanye Tawwaf ya Al Kaabah hadi pale utakapotoharika kutokana na Hedhi.’*(Sahih Al Bukhari)*

Na amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua**:**

حاضتْ صفيّةُ بنتُ حُييّ بعد ما أفاضتْ ، قالت عائشةُ : فذكرتُ حيضتَها لرسولِ اللهِ صلى الله عليه وسلم ، فقال رسولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم أحابستُنا هيَ ؟ فقلتُ يا رسولَ اللهِ : إنها قد كانتْ أفاضتْ وطافتْ بالبيتِ ، ثم حاضتْ بعد الإفاضةِ ، فقال رسولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم : فلتنفِرْ

‘Safiyyah Bint Huyayy aliingia kwenye Siku zake baada ya Kufanya Ifadah. Hivyo nikamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Hedhi yake*, na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Atatufanya tuwe wenye Kumsubiri?’

Hivyo Mimi nikasema: ‘La Ya Rasul Allah kwani ameshafanya Tawaf Al Ifadah na ndio akapata Hedhi.’

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam akasema: Basi mwachie afunge Vitu Aondoke pamoja nawe.’(Sahih Bukhari)*

Ifadah humaanisha kuwasili kwa Mahujaji kutoka katika Mina na Arafa kuingia kwenye Mji wa Makkah, katika siku ya Idd Al Adhha na Kufanya Tawwaf mara 7 kuzunguka Al Kaabah ambayo hua ni Nguzo ya Hijja na huitwa *Tawwaf Al Ifadah.*

Ambapo Hadith hii inaonesha kua Mwanammke asiekua Tohara kabla ya *Tawaf Ifadah* basi anatakiwa asubiri hadi atoharike kisha ndio afanye *Tawwaf Ifadah* na hivyo itambidi asubiri asiondoke Makkah.

Na pia amesema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua**

الطوافُ بالبيتِ صلاةٌ إلا إنكم تتكلَّمونَ فيه

Tawwaf katika Bayt ul Allah hua ni Sala isipokua inaruhusiwa kuzungumza ndani yake.’*(Imam At Tirmidhi, Imam Ibn Hibban, Imam Ad Darimi, Imam At Tabarani)*

Ambapo hii inathibitisha kua Tawwaf hua ni Sawa na Hukmu za Sala isipokua ndani yake mnaruhusiwa Kuzungumza, Kutembea, n.k.

Na anasema Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua: **‘Jambo Muhimu katika Tawwaf ni kua Mtu anatakiwa awe ni mwenye kujishughulisha na kumkumbuka *Allah Subhanah wa Ta’ala*, na kusoma Qur’an kaika wakati huo, na hua inaruhusika kuzungmza isipokua kutozungumza hua ni bora zaidi, kwani Abd Allah Ibn Mubarrak alikua akisema kua: ‘Hakuna Jambo zuri zaidi**

katika Tawwaf kama kusoma Qur'an. Na Mujahid alikua akifanya hivyo pia na Imam Al Shafii na Abu Thawr alikua akipendekeza hivyo.'

Na yeyote yule anaeruhusu kusomwa kwa Qur'an njiani, na Jangwani na kisha akaikataza katika wakati wa Tawwaf basi hua hana kithibitisho'*(Tuhfat al-Muhtaj, Nihayat al-Muhtaj)*

Hivyo hadith hizi zinathibitisha kua Moja kati ya Masharti ya Kukubalika Tawaf ni Tohara ya Kua na Udhu, ambapo huo ndio pia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik, Imam Al Shafii na pia Mtizamo wa Imam Malik.

Kama anavyosema Shaykh ul Islami Imam Abu Zakarriyah An Nawawi kua**: 'Imam Al Mawardi amenukuu juu ya hili kutoka kwa wengi miongoni mwa Wanazuoni na Imam Ibn Al Mundhiri amenukuu pia kuhusiana na Udhu katika Tawwaf kutoka kwa Wanazuoni wengi**.'(*Al Majmuu)*

Hivyo Wengi Miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal ni wenye kukubaliana kua : '**Kua Tohara kutokana na Hadathi kubwa na Hadathi ndogo hua ni Sharti la Kukubalika kwa Tawwaf za aina zote**. **Iwe *Tawaf Al Qudum* (ya Maamkizi), *Tawaf Al Ifada* (ya Hija), *Tawaf Al Wadaa* (ya Kuaga), Tawaf ya Umra au Tawaf ya Sunnah, hivyo kama Mtu akiwa Hana Udhu katika wakati wa Kutufu basi Tawwaf yake hua ni Batili na haihesabik**i.'*(Sharh Al Kabir Imam Ad Dardi Al Maliki, Nihayat Al Muhtaj Imam Al Ramli Al Shafii, Mughni Al Muhtaj Imam Al Shirbini Al Shafii na Al Insaaf Imam Al Mardawi Al Hanbali)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Ala Ad Din Al Kasani Al Hanafi basi yeye anasema kua: '**Kua na Udhu hua si Sharti la kukubalika kwa Tawaf, mbali ya kua ni Wajib kua na Udhu Hivyo kama Mtu atafanya Tawwaf bila kua Tohara, basi hua ni Wajibu kwake kuirudia Tawaf hio wakati akiwa katika Mji wa Makkah au vyenginevyo basi itambidi Atoe Kafara'***(Badai Al Sanai Fii Tartib Ash Sharai)*

Ambapo kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi maana ya kuirudia *Tawwaf* hua ni kuirudia *Tawwaf* yote tangu mwanzo hadi mwisho. Lakini hata hivyo kama ikiwa Mtu atatia Udhu kisha akafaya *Tawwaf* na kisha Udhu ukamtoka katikait ya *Tawwaf* basi Mtu huyo hua anaruhusika kumalizoia *Tawwaf* yake hio.

Na pia kwa Mtu ambae atafanya *Tawwaf* bila kua na Udhu halafu katikati akaamua kutia Udhu basi hua anaruhusika kumalizia *Tawwaf* yake bila kurudia *Tawwaf* alizofanya kabla ya kua na Udhu. Kama anavyosema Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa, Imam Muhammad Ibn Al Hasan kua: '**Amesema Imam Abu Hanifa kua, Kama ikiwa Mtu atahisi kubatilika kwa Udhu wake wakati akiwa anazungunguka Al Kaabah, au akiwa katika Kukazana baina ya Safa na Marwa, au akiwa baina yake sehemu hizo, na kisha ikamtokea hali hio huku akiwa ameshafanya baadhi ya *Tawwaf* au *Tawwaf* zote, lakini hajasali Rakaa mbili bado za baada ya *Tawwaf*, basi itambidi Kutia Udhu na kisha kuendelea kumalizia *Tawwaf* yake na kusali Rakaa mbili baada yake kama akitenguka Udhu basi itambidi atie Udhu kisha aendelee na Tawwaf yake.'***(Al Hujjah Alaa Ahl Al Madina)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Kasani anaendelea Kusema kua: **'Hivyo Kuhusiana nasi (Wafuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa) basi Tohara ya kutokana na Janaba, Hedhi, Nifasi, na Kutia Udhu hua si Wajibu katika kukubalika Kufanya Tawwaf, bali hua ni Wajibu na hivyo Hua inakubalika Kufanya *Tawwaf* bila kutia Udhu. Ama kulingana na Imam Al Shafii basi hua ni Sharti kua na Tohara hivyo Tawwaf haikibaliki bila kua Tohara.**

Na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: '*Tawwaf* ni Sala, isipokua Allah ameruhusu Kuzungumza Ndani yake. Na hivyo Kama *Tawwaf* ni Sala basi hua hairuhusiki Kuifanya Bila Tohara. Ambapo sisi (Mahanafi) tuna uthibitisho wa Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo:

﴿ثُمَّ لْيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ﴾

Thumma lyaqdhoo tafathahum walyoofoo nudhoorahum walyattawwafoo bialbayti alAAateeqi. *(Surat Al Hajj 22:29)*

Tafsir: **Hivyo Wache Wamalize Majukumu ya Hijja juu yao na watumize Nadhiri Zao Na wafanye Tawwaf *(Al Ifada)* Katika Nyumba ya Kale *(Kaabah).***

Ambapo hii ni Aya inayoamrisha Kufanya *Tawwaf* bila ya kuwepo kwa Sharti la Kua Tohara, hivyo hua hairuhusiki Kuliwekea Mipaka jumlisho la Aya kutokana na Hadith moja Peke yake. Na hivyo hadith hii hutafsiriwa kua kama mithili yake, yaani kama vile alivyosema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿ٱلنَّبِيُّ أَوْلَىٰ بِٱلْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنفُسِهِمْ وَأَزْوَاجُهُ أُمَّهَاتُهُمْ﴾

Alnnabiyyu awla bialmu/mineena min anfusihim waazwajuhu ommahatuhum *(Surat Al Ahzab 33:6)*

Tafsir: **Nabii Muhammad (*Salallahu Alayhi wa Salam*) Yuko karibu sana na Waumini Kuliko Wao Waumini Wenyewe na Nafsi zao Na Wake Zake ni Mama Zao(Waumini).**

Yaani wake wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Kama Mama zao Waumini, hivyo *Tawwaf* hua ni kama Sala yaani katika Malipo au katika wajibu wa *Tawwaf* ya Hajj kwa sababu neno Kama hua halina Mjumuisho, hivyo hua linatafsirika kwa upande mwengine kama Mithili yake, na hii ni kulingana na Qur'an na Hadith.

Yaani au tunaweza Kusema kua *Tawwaf* hua ni Sawa na Sala Lakini hua si Sala, na kutokana na kua Si Sala, basi hua hakuna Ulazima wa Kua na Udhu. Na pia kutokana na kua ni Mithili ya Sala basi Udhu hua unahitajika juu yake, na hii ni kulingana na Vithibitisho Viwili hivi hua inawezekana kua hivyo.

Hivyo ijapokua Udhu hua unahitajika katika *Tawwaf,* lakini kama mtu akifanya *Tawwaf* bila ya Udhu wakati akiwa katika Mji wa Makkah, basi humbidi kuirudia *Tawwaf* hio. Kwa sababu kuirudia hua ni sehemu ya kulipa Kwa kitu mithili yake na kulipa kitu kwa mithili hua ni bora zaid, kwa sababu kufanya hivyo hua ni kukamilisha kinacholipwa.

Hivyo kama Mtu akirudia katika Siku za Kuchinja basi hua hakuna tatizo lakini kama akichelewasha basi itambidi kutoa Fidia kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Hanifa.'*(Badai Al Sanai Fi Tartib Ash Sharai)*

Na anasema Imam Abu Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Rushd Al Andalus Al Maliki kua: '**Ingawa Wanazuoni Wametofautiana kuhusiana na Kuruhusika kufanya Tawwaf bila ya kua na Udhu,**

lakini hata hivyo Wanakubaliana kua Kua na Udhu hua ni moja kati ya Sunnah zake.'*(Bidayat Al Mujtahid wa Nihayat Al Muqtasid)*

Ambapo amesema Imam Abu Thawr Al Shafii kua: '**Kama ikiwa Mtu atafanya Tawwaf bila ya kua na Udhu, basi Tawwaf yake itamtosheleza kama ikiwa hajui kua alikua anatakiwa atie Udhu, lakini kama akiwa anajua basi Tawwaf yake hua mi Batil.'***(Tuhfah Al Muhtaj)*

Na anasema Imam Ibn Aabidin Ash Shaami Al Hanafi kua: '**Amesema Ahu Hanifa kua kama ikiwa Mtu atafanya Tawwaf bila ya Kua na Udhu basi Itamtosheleza na inapendekezwa kua airudi**e.'*(Khashiyah Ibn Aabidin)*

Na Al Allamah Imam Ahams Ad Din Muhammad Ibn Muhammad Ash Shirbini Al Shafii anasema kua: '**Kama Mtu akibatilisha Udhu wake kwa Makusudi katika Tawwaf, basi hua anatakiwa akatie Udhu na hua ni bora zaidi kama akikoga Janaba kabisa. Na kisha arudi kwenye Tawwaf kwa kuanzia katika Sehemu aliyojibatilisha Udhu wake, iwe kwenye Pembe ya Al Kaabah ama la, na kuna Mtizamo usemao kua ni bora kuanza Upya, kama ilivyokua kwenye Sala.**

Hivyo kama kizuizi husika kitaondolewa au kitarekebishwa basi Mtu husika ataanza aliposimamia baada ya kuzuilika, kama vile ilivyokua katika Sala. Isipokua Tofauti ni kua Tawwaf Hua inaweza kujumuisha kile ambacho hakiwezekani ndani yake, kwa mfano kama ikiwa Nguo, Mwili au sehemu ya Tawwaf ina Najis ambayo hairuhusiki kuidharau, au kama ikiwa sehemu ya Mwili inayotakiwa kufunikwa Imekua wazi, au Nywele za Mwanamke zinaonekana, au Kucha ya Kidole chake inaonekana basi kitendo husika kitakua ni batili.

Hivyo kama kizuizi husika kitaondolewa au kitarekebishwa basi Mtu husika ataanza aliposimia kwa kuzuilika, kama vile ilivyokua Kwa Mtu alietokwa na Udhu, iwe umepita mda mfupi au mrefu, kwa sababu hua hakuna sharti la kusimamia utaratibu wah atua za kimpangilio kama ilivyo kwenye Kutia Udhu.

Kwa sababu vyote ni vitu ambavyo vinaweza vikaingiliana na na vitu ambavyo havihusianai navyo, na hivyo Tawwaf hua ni tofauti na Sala, lakini hata hivyo kwa Tawwaf basi hua inapendekezwa kuanza upya ili kujitenga na tofauti za Mitizamo ya Wanazuoni waliosema kua hua ni wajibu.*(Mughni Al Muhtaj)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Dardir Al Maliki basi anasema kua: **'Mtu atakaetokwa na udhu wakati akiwa katika Tawwaf basi hua anatakiwa kuanza Upya Tawwaf yake, na wala hatotakiwa kuendelea kutoka katika sehemu aliyokatikiwa na Udhu ndani yake.'***(Sharh Al Kabir)*

Na akasema Imam Al Kharashi Al Maliki kua: **'Tawwaf hubatilika kutokana na kitendo cha Makusudi au cha kusahau**. **Yaani kama Mtu akisahau kua Yupo kwenye Tawwaf basi Tawwaf yake itabatilka na hivyo Ambapo kwa Upande wa Imam Al Dardir Al Maliki basi anasema kua: Mtu atakaetokwa na udhu wakati akiwa katika Tawwaf basi hua anatakiwa kuanza Upya Tawwaf yake, na waka hatotakiwa kuendelea kutoka katika sehemu aliyokatikiwa na Udhu ndani yak**e.'*(Sharh Al Kabir)*

Na akasema Imam Al Kharashi Al Maliki kua: Tawwaf hubatilika kutokana na kitendo cha Makusudi au cha kusahau. Yaani kama Mtu akisahau kua Yupo kwenye Tawwaf basi Tawwaf yake itabatilka na hivyo Hatoruhusika kuanza alipomalizia bali atatakiwa kuanza Mwanzo. Na hii ni kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu, na Hivyo Tawwaf ya Wajib huanzia kwa Kutia Udhu,ila si kwa Tawwaf ya Sunna. Na Mtu akitokwa na Udhu kisha akatia Udhu na kuendelea

pale aulipokatikia bila kuanza Mwanzo basi Tawwaf yake hua ni Batili kulingana na mtizamo wa Ibn Qasim ambao ni tofauti na Mtizamo wa Ibn Habib.'(*Sharh Mukhtasar Al Khalil)*

Ambapo Imam Ad Dardir anamalizia kwa kusema kua: **'Ingawa hairuhusiki kuendelea na Tawwaf baada ya kunatilika kwa Udhu bila kuanza upau lakino kama ikiwa Mtu atatokwa na Damu ya Pua, basi ataruhusika kutia Udhu kisha kuendelea na Tawwaf pale pale katika sehemu ulipomkatikia Udhu, kama ikiwa sehemu hio na ya kutilia Udhu itakua sio mbali na pia ikiwa hakukanyaga Najis njiani.'***(Sharh Al Kabir)*

Na akasema Imam Al Buhuti Al Hanbali kua: **'Mtu akitokwa na Udhu katika Tawwaf iwe kwa makusudi au kwa bahati mbaya basi atatakiwa kuirudia Upya Tawwaf hio'***(Sharh Al Muntaha)*

Na akasema Ima. Al Mardawj Al Hanbali kua: **'Kama Mtu akitokwa na Udhu katika wakati wa Tawwaf au ameikatisha Tawwaf kwa mda basi atatakiwa kuanza Upya Tawwaf yake hio'***(Al Insaaf)*

Naam anasema Al Hafidh Imam Abu Bakr Ibn Muhammad Ibn Abi Shaybah Ibn Ibrahim Ibn Uthman Al Kufi kua
Amesema Ghundar kua amesema Shu'bah kua: Niliwauliza mimi Al Hakam, Hammad, Mansur na Sulayman kuhusiana na Mtu anaefanya Tawwaf katika Al Kaabah huku akiwa hana Udhu, ambapo nao wakasema kua: Hakuna Tatizo*(Musannaf Ibn Ani Shaybah)*

Na anasema Imam Abu Hasan Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii kua: '**Tohara katika Kufanya Tawwaf hua Wajjibu na ni Sharti la Kukubalika ni Mtu kua Tohara na kutokua na Najis,na hivyo kama Mtu akifanya Tawwaf bila kua Tohara basi Tawwaf yake hua ni Batili. Na huu ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanafiqh.**

Isipokua Abu Hanifa ambae amesema kua Tohara hua ni Wajib kwa afanyae Tawwaf, Lakini Tohara hua si Sharti la Kukubalika kwa Tawwaf Hivyo kama Mtu akifanya Tawwaf bila kua Tohara, na kisha akawa yuko katika Mji wa Makkah, basi itambidi airudie Tawwaf hio. **Lakini kama ikiwa amesharudi nchini kwake basi Tawwaf yake humtosheleza ila atatakiwa achinje kwa ajili ya kutoa Fidia.'***(Al Hawi Al Kabir)*

Hivyo hapa tunakumbushana tena kua kwa Upande wa Madhhab yote tunaona kua Wakisema kua Hukmu ni Wajib basi hio hua inamaanisha kua Fardhi au Lazima na hivyo haitakiwi kuacha kwani ukiwacha Basi umebatilisha Ibada husika. Lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao hua wana Hukmu mbili tofauti, kwanikuna Hukmu ya kua ni Wajib na Kuna Hukmu ya kua ni Fardhi.

Yaani Kitu kikiwa Wajib basi kama Kiikachwa hua hamna tatizo na Ibada haibatiliki, ila ni bora zaidi kufanya na kitu kikiwa Fardhi basi hua ni Lazima na Hakifai kuachwa kwani kikiachwa basi Ibada husika hubatilika.

Na ndio maana tunaona kua Imam Abu Hanifa akasema kua Udhu kwa Tawwaf ni Wajibu lakini si Lazima.

Na tunaporudi kwa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi basi yeye anasema kua: '**Al Shafii amesema kua Tohara ni Sharti kwa Tawwaf zote.'**

Imam An Nawawi anaendelea kusema kua: '**Na hivi ndivyo Wanazuoni wetu wote wanavyokubaliana, na hakuna kutokukubaliana isipokua kwa kuwepo Mtizamo Dhaifu usiokua na Nguvu ambao ni Mtizamo wa Imam Abu Yaqub na wengineo Kupitia kwa Imam Al Haramayn ambae amenukuu kua kutoka kwa baadhi ya Wanafiqh wetu wamesema kua Tawwaf Al Ifadah hua inakubalika bila ya Mtu kua na Udhu.'***(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Hivyo tunamalizia baada ya kuangalia Mitizamo ya Madhhab mbali mbali na ya Wanazuoni mbali mbali wa Fiqh kuhusiana na Hukmu ya Tawwaf na Udhu kwa vithibitisho vyao kulingana na Mitizamo yao.

Na hivyo tunahitimisha kwa kusema kua Madhhab yote yanakubaliana kua Udhu katika Tawwaf ni Wajib na hivyo kua ni sharti na nguzo ya Tawwaf ma Tawqaf haikubaliki bila Udhu isipokua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambao Wanasema kua Udhu katika Tawwaf hua ni Wajibu lakini si Sharti, na Hivyo Tawwaf inakubalika bila ya Udhu ila itabidi Mtu atoe fidia.

Na pia kuna Wanazuoni ambao Mtizamo wao unahesabika kua ni Dhaifu na hauna nguvu kua Udhu katika Tawwaf hua si Lazima.

Na tumeyazungumzia yote haya baada ya kuzungumzia Kubatilika Udhu kwa Kugusana baina ya Mwanname na Mwanamke kwa sababu ya kutaka kujua kuhusiana na Udhu katika Tawaf kulingana na Hali ya Ibada ya Hija katika wakati wetu ambapo Mamilioni ya Watu Wanaume na Wanawake Wanasongamana, Jee Udhu utabatilika ama la.

Hivyo baada ya Kuangalia kuhusiana na Udhu na Kugusana na Ajnabi kua kuna Mtizamo Mitatu Ifuatayo:

1-Udhu Unabatilika kwa Kugusana na Mwanamke Ajnabi iwe kwa Matamanio ama La, iwe kwa Kusahau, kwa Makusudi Ama La, ambapo huu ni Mtizamo Unaokubalika na Kutegemewa na katika Madhhab ya Imam Al Shafii.

2-Udhu Haubatiliki kwa Kugusana Na Mwanamke yeyote, hata kwa matanio ila Utabatilika pale itakapokua Tayari Mwanammke na Mwanamme husika Wanataka kuingiliana Kimwili.

3-Udhu Haubatiliki kwa Kugusana na Mwanamke isipokua kama itakua kuna Matamanio baina yao.

Na baada ya kupata Mitizamo hii basi tukaanngalia kuhusiana na Tawwaf na kuona kua kulingana na Madhhab ya Imam Al Shafii, Madhhab ya Imam Malik na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kua Udhu hua ni Sharti la kukubalika kwa Tawwaf Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi Wao Wanasema kua Udhu hua ni Wajib tu na wala ai Sharti la kukubalika kwa Tawwaf.

Hivyo bila ya Shaka tunapochukua Hukmu hizi mbili na na kuzisimamia kulingana n Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi si Katika Ibda ya Hija wala Umra ambayo itakubalika kwa sababu Haiwezekani kufanya Tawwaf bila Kugusana na Wanawake Ajnabi ambao nao watakutoa Udhu na kukubatilishia Tawwaf yako.

Hivyo kutokana na Mashakil haya basi kwa baadhi ya Wasiojua wanawaweza wakasema kua hapa baada ya Kutia Udhu basi itabidi tufuate Mtizamo wa Imam Abu Hanifa au Imam Malik au Imam Ahmad Ibn Hanbal, ili hata ukigusana na Mwanamke basi Udhu usitoke, kama hujamtamani n.k

Na ingawa kufanya hivyo hua ni kujiondolea Mashakil na hivyo kurahisisha njia ya kufanya Ibada lakini hata hivyo kwa upande wa Kifiqh basi hua hairuhusiki kuchanganya Hukmu za Madhhab mawili Tofauti katika Ibada moja, au Maimamu wawili tofauti katika Ibada moja ambapo Kufanya hua kunajulikana kama kufanya Talfiq.

Yaani Talfiq hua ni Kuchanganya Mitizamo ya hukmu mbili tofauti katika Ibada moja na hivyo Mtu kua ni mwenye kupata Mchanganyiko wa Hukmu ambao haukubaliki na Madhhab yote mawili aliyoyachanganya Hukmu zake.

Kwa Mfano Mtu tuchukulie mtizamo wa Udhu, kwa Mtu katika Udhu wake Kufuata Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua Udhu wake haubatiliki atakapogusana na Mwanamke,na kisha akagusana na amwanamke njian na akaenda kusali lakini wakati anasali akajikuta kua ametoka Damu, na kulingana na mtizamo wa Imam Abu Hanifabasi Udhu wake utakua umebatilika na Sala yake pia. Lakini Mtu huyo akaamua kuendelr kusali kwa kufuata Mtizamo wa Imam Al Shafii kua Udhu wake haujabatilika.

Hivyo katika hali kama hii basi atakua ni mwenye Kubatilisha Ibada ya Sala yake, kutokana na kua Ametumia Hukmu mbili tofauti ambazo ndani ya Ibada yake, kiasi ya kua Hakuna Hata Mmoja kati ya Maimamu wawili hawa atakaesema kua Sala ya Mhusika imesihi,

Kwani wanasema Wanafunzi wawili wa Shaykh Ul Islami Imam Zakarriyh Al Ansari ambao ni Shaykh Ul Islami Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Misri L Ansari Shams Ad Din Al Ramli Al Shafii na Shayk Ul Islami Imam Al Muhaqqin Shihab Ad Din Imam Abu Abbas Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: 'Kwa Yeyote yule anaemfuata Imam wake wa Madhhab katika Jambo basi anatakiwa afuate kila kitu kinachohusiana na Jambo husika kulingana na Mtizamo wa Skuli ya Fiqh ya Madhhab yake' *(Ianat At Talibin)*

Naam, baada ya kuangalia Udhu na Tawwaf basi tumeona kua labda Mtu afanye Talfiq, yaani kuchanganya Hukmu za Madhhab tofauti katika Ibada, ili Tawwaf yake ikubalike katika Ibada ya Hja lakini hata hivyo tunaona kua haikubaliki kwani kuna tofauti baina ya Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Abu Hanifa katika mambo kadhaa kwa mfano.

1-Kuhusiana na Udhu, ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua Lazima Mtu afuate Utaratibu wa hatua za Kutia Udhu, lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wanasema kua hakuna Ulazima huo.

Pia kuhusiana na Kupaka Maji kichwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wanasema kua Inatakiwa Kupaka Maji Kichwani Japo Kidogo yaani Japo sehemu ya Nywele Moja ya Kichwani ikiguswa na maji basi itatosheleza katika Kutia Udhu.

Ambapo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa wao wanasema kua Ili Udhu Ukubalike basi Lazima eneo la Kichwa utakalolipaka Maji katika Udhu lisipungue Robo ya kichwa, hivyo ikipingua basi Udhu hua ni Batili.

Ama kuhusiana na Ibadah ya Hija basi pia kuna Tofauti zifuatazo:

1-Niyyah na Talbiyah ya Hajj hua ni Lazima wakati mtu anapoingia kwenye Ihram.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi Mtu anapoingia kwenye Ihram hua anahitaji Nia tu, kwani Talbiyah si lazima.

2-Madhhab ya Imam Abu Hanifa hayaruhusu Mtu kuingia katika Ihram kabla ya kuwasili katika Mikat au sehemu ya Kuingia Ihram.

Madhhab ya Imam Al Shafii inaruhusu kuingia kwenye Ihram: Kabla Kuwasili kwenye Miqat.

3-Kujipaka Manukato mwilini kabla kuingia kwenye Ihram hua inaruhusika, lakini kujipaka Ihram hua hairuhusiki.

Katika Madhhab ya Imam Al Shafii inaruhusika Kujipaka manukato Mwilini na Kwenye Ihram pia, lakini kwenye Ihram inabidi utie manukato baada ya kutia nia, kwani ukiitia Manukato Ihram baada ya kutia nia basi hua hairuhusiki kuivaa Ihram husika hadi itakapofuliwa na kutonuia manukato hayo.

4-Madhhab ya Imam Abu Hanifa Kutumia Pini au Vifungo kwa ajili ya Izar au Nguo Ya chini lakini katika Nguo ya Juu hua haipendekezwi.

Katika Madhhab ya Imam Al Shafii haikubaliki kutumia Pini bali inakubalika Kutumia Kifungo au Kamba, na Nguo ya Juu hua hairuhusiki Kuifunga.

5-Tawwaf kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa hua ni Lazima kutembea kwa Miguu, kama Mtu anaweza, hivyo kama Mtu akifanya Tawaf juu ya amepanda Kipando basi hua ni lazima Kutoa Fidia kaa kutotekeleza Wajibu wa Ibada ya Hija.

Madhhab ya Imam Al Shafii Ni Sunnah kutembea kwa Miguu katika Tawwaf Kwa anaeweza na haipendekezwi kupanda Kipando katika Tawwaf, hivyo Mtu akipanda Kipando basi itabidi alipe fidya.

6-Tawwaf ya Ufunguzi kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa hua ni Wajibu kuanzia katika Hajar Al Aswad, hivyo mtu akianza mbele yake basi hua haikubaliki hesabu ta Tawwaf yake hadi aanze kwenye Hajar Al Aswad.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii Tawwaf ya Ufunguzi hua ni Lazima, Fardhi kuanzia Kwenye Hajar Al Aswad na hutakiwi kuikosa kwa sababu hua haina fidia badala yake.

7-Tawwaf Al Ifadah kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa hua ni Lazima katika Wakati wa Baada ya Sala ya Alfajir ya Siku ya Idd Al Adhha tu, Hivyo haikubaliki kuifanya baada ya wakati huo, ingawa inakubalika kufanya Kabla ya wakati huo lakini haipendekezwi na hua ni Sunna kuifanya baada ya kurusha Mawe na Kunyoa.

Katika Madhhab ya Imam Al Shafii hua inaruhusika Kufanya Tawwaf Al Ifadah kabla ya Salat Al Fajr katika Siku ya Idd Al Adhha, na haipendekezwi kufanywa nje ya Wakati wake uliowekwa.

8-Madhhab ya Imam Abu Hanifa hua hairuhusiki kukatisha mpangilio wa hatua baina ya Tawwaf na Sa'i isipokua kama itakua kuna Dharurah.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua ni Wajibu kuendeleza Mpangilio wa hatua baina ya Tawwaf na Sa'i,na kama kuna dharurah basi inakubalika kukatisha na kuendelea baadae Ambapo Kukatisha huko hua hakuhesabikikua ni Kukatisha.

9-Wakati wa Kukaa Muzdalifa kwa Upande wa Madhhab ya Ima. Abu Hanifa mwisho wake hua ni baina ya Alfajir hadi kuchomoza Jua, ukizidisha bila dharura baso utalipa fidya.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wakati wa Kukaa Muzdalifa huanzia Usiku wa Manane hadi Alfajir, hivyo kukaa hata kwa Dakika kadhaa hua kunatosheleza, ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal.

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua wakati wa kua Muzdalifa ni kuanzia Magharibi ya Siku ya Arafah hadi Alfajir.

9-Kuchanganya Isha na Magharibi katika eneo la Muzdalifa hua ni Lazima na ni Nguzo ya Ibada ya Hija kwa Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao Wanasema kua Kuchanganya Maghrib na Isha katika Muzdalifa hua si Wajib bali kunapendekezwa.

10-Kulala Minna katika Siku za Tashrik hua Inarahisisha kupiga Mawe, jambo ambalo hua si sharti la Ibada ya Hija hii ni Kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii Kulala Minna katika Siku za Tashrik hua ni Wajibu, hivyo asielala basi atalipa Fidya.

11-Kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi hua hakuna ulazima wa Kupangilia utaratibu wa kupiga Mawe katika Jamarat Tatu.

Katika Madhhab ya Imam Al Shafii hua ni Wajibu kupiga Mawe katika Jamrat kwa mpangilio, hivyo ukikosea basi itabidi urudie upya.

12-Sai ya Safa na Marwa hua ni Wajibu kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa hivyo ukidharau basi utalipa Fidya, na Sa'i lazima ifanywe kabla Tawwaf ikifanywa baada basi Tawwaf hua batili.
Kwa Madhhab ya Imam Al Shafii Sai baina ya Safwa na Marwa hua ni Nguzo ya Hija na Umra ukiidharau basi Hija/ Umra imebatilika.

13-Kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa Sa'i inaweza kufanyaa kabla ya kwenda Arafah baada ya kufanya Tawwaf ya Sunnah.

Madhhab ya Imam Al Shafii hua hairuhusiki kufanya Sa'i kabla ya Arafah.

14-Madhhab ya Imam Abu Hanifa hua inaruhusika Kufanya Sa'i chini ya Mizunguko 7 , yaani japo mara 3 kama huwezi kisha utatoa Sadaqah.

Madhhab ya Imam Al Shafii ni lazima kutimiza Idadi ya mizunguko 7 kwa sababu Sa'i ni Nguzo ya Hija.

15-Madhhab ya Imam Abu Hanifa Kunyoa/Kukata Nywele hua kunajumuisha Kichwa kizima na Mwisho wa Kunyoa ni Maghribi ya Mwezi 3 Dhul Hijjah, na hivyo kama ukipitisha zaidi ya mda huo utalipa Fidya.

Madhhab ya Imam Al Shafii Kunyoa Kichwa kiIma hua ni Sunna, lakini inakubalika hata kukata Nywele 3 tu, na inapendekezwa mwisho wa kunyoa kua ni katika Magharibi ya Mwezi 3 na ingawa si Wajibu, lakini hutoweza kutoka kwenye Ihram hadi unyoe.

16-Kunyoa Hua ni Vizuri kabla Tawwaf Ifadah kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii hua ni baada ya Tawwaf Al Ifadah.

Naam..hizo ni baadhi ya Tofauti za Madhhab katika Udhu na Ibada ya Hija, jambo ambalo linatuwekea wazi kua Ukichanganya Mitizamo basi utakua huna Ibada ya Hija.

Hivyo kama tunavyoona kua kuna tofauti kadhaa baina ya Mitizamo ya Madhhab kuhusiana na Ibada ya Hijja na pia kuhusiana na Udhu, jambo ambalo kinatuwekea wazi ni kwa sababu gani Wanazuoni wakasema kua hairuhusiki Kufanya Talfik katika Ibada kwani hua ni sawa na Mtu Kufuata Urahisi wa Matamanio ya Nafsi yake katika Ufanyaji wa Ibada Husika.

Kwani amesema Shaykh Ul Islami, Imam Al Muhaqqiqiin Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua; '**Hua ni Sharti kutochanganya Mitizamo ya Skuli tofauti za Madhhab (Talfiq), kama ikiwa Mtu atataka Kufuata au kujumuisha sehemu ya Jambo kwa kumfuata Imam wa Madhhab mengine, na hii ni kwa sababu imethibitishwa kua Kufanya Talfiq imeharamishwa.**

Yaani kwa mfano Mtu kufuata Mtizamo Madhhab ya Imam Malik. Kuhusiana na Utohara wa Mbwa na kisha hapo hapo akatia Udhu kwa Kutumia Njia ya Mfumo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kwa Kukosha sehemu tu ya Kichwa. Hivyo Juu ya hili basi kuna makubaliano ya Kutokukubalika kwake.'*(Fatawwa Al Fiqhiyyah Al Kubra)*

'Hivyo basi Kufanya Talfiq hua hakuruhusiki kwa Mtu asiekua na Kuhusiana na Utohara wa Mbwa na kisha hapo hapo akatia Udhu kwa Kutumia Njia ya Mfumo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kwa Kukosha sehemu tu ya Kichwa.Hivyo Juu ya hili basi kuna makubaliano ya Kutokukubalika kwake.'*(Fatawwa Al Fiqhiyyah Al Kubra)*

Hivyo basi Kufanya Talfiq hua hakuruhusiki kwa Mtu asiekua na Ilm ya tofauti baina ya Mitizamo ya Madhhab juu ya Jambo husika. Ila kama ikiwa Mtu anayo Ilm hio basi bila ya Shaka hua inaruhusika, hususan pale inapokua kuna Ugumu wa Kushikamana na Hukmu za Madhhab fulani katika Jambo husika.

Kwa mfano kutokana na kua Tawwaf inahitajia Udhu kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa hua Haihitaji udhu, basi ili kuepuka mashakil basi Kwanza unatakiwa Ujue Masharti ya Udhu kulingana na Mtizamo wa Madhahab ya Imam Abu Hanifa kisha Utie Udhu kama Mfuasi wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Na hivyo kwa kua umetumia mfumo wa Udhu wa Imam Abu Hanifa basi kwako Udhu hautobatilika hata kama ukigusana na Mwanamke Ajnabi. Na hivyo basi utaruhusika kufanya Tawwaf kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii. Kama tutakavyoona hapo baadae, ila kabla ya Kuendelea basi tumkamate Imam Al Muhaqqiqin Imam Shihab Ad Din Abu Abass Ahmad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii ambae anatuambia kua:

‘Inaruhusika kwa Mufti -Mwanazuoni anaejua Hukmu za Sharia- Kutoa Fatwa kulingana na Madhhab yake au Kulingana na Madhhab mengineyo kama ikiwa anafahamu Msingi wa Hukmu Husika katika Madhhab Husika juu ya Jambo Husika.’*(Fatawwa Al Fiqhiyyah Kubra)*

Hivyo basi ili Mufti au Mtu husika aruhusike kuachana Na Mtizamo wa Madhhab yake katika Jambo Husika na kufuata Mtizamo wa Madhhab mengine basi inatakiwa kuwepo kwa haoi zifuatazo:

1-Madhhab husika lazima yawe na Maelezo ya Mfumo kamili wa Hukmu zake za Fiqh, Jambo ambalo litampelekea Mtu anaetaka kufuata kua na Uhakika wa Hukumu Husika juu ya Jambo husika.

2-Mtu Husika lazima awe anajua na Kufahamu Hali ya mazingira na Masharti yanayohusiana na Jambo husika analolitafutia Fatwa yake katika Madhhab Husika.

3-Mtu husika anatakiwa asiwe ni mwenye Kutafuta Urahisi wa Jambo husika kutokana na kua na Uvivu juu ya Jambo Husika.

Kwani anasema Shaykh ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: ‘Kama ingekua inaruhusika kwa Mtu kufuata Madhhab anayotaka katika Kila Jambo, basi ruhusa hii ingepelekea kuwepo kwa Uvivu juu ya Mitizamo tofauti ya Madhhab kulingana na Matamanio ya Mtu husika, na hivyo Watu wangekua wanakwepa na Kuzunguka zunguka baina ya Yaliyoruhusiwa na yaliyokatazwa baina ya Madhhab tofauti, na yaliyokua ya Lazima na yaasiyokua na ulazima baina ya Madhhab tofauti na hivyo hii ingepelekea Kuvunjika kwa Umoja wa Mshikamano wa Utekelezaji wa Majukumu ya Kidini kwa Ujumla.

4-Mtu husika anatakiwa awe na Uhakika kua anachokifanya katika kuachana na Mtizamo wa Madhhab husika hakitapelekea kusababisha Talfiq.

5-Lazima kuwe na Ulazima unaokubalika kisharia kwa Mtu husika Kuachana kufuata Mtizamo wa Madhhab husika kutokana na Dharurah husika. Na Hivyo Mtu husika anatakiwa ajue na kuweza kutofautisha baina ya Umuhimu wa Hitajio la Mtu mmoja kuachana na Mtizamo wa Madhhab husika na umuhimu wa Hitajio la Mufti anaefuatwa na Watu kuachana na Mtizamo wa Madhhab husika katika Jambo husika.
Kwani Mtu hua anatakiwa kushikamana na Mtizamo wa Mufti husika katika Jambo husika kwa ajili ya Maslahi ya Jamii ya watu husika katika eneo husika juu ya jambo husika.

Na miongoni mwa mifano ya mambo ambayo yanakubalika kwa mtu kuachana na Mtizamo wa Madhhab yake kutokana na Dharurah ambayo inaweza kuwepesishwa kwa kufuata Mtizamo wa Madhhab mengine ni kuhusiana na Zakkat.

Jambo ambalo wengi wetu wamekua wakilaumiana kuhusiana na Ugawajwi wake ambao umeainishwa kwenye Qur'an katika aya isemayo:

﴿إِنَّمَا ٱلصَّدَقَاتُ لِلۡفُقَرَآءِ وَٱلۡمَسَاكِينِ وَٱلۡعَٰمِلِينَ عَلَيۡهَا وَٱلۡمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمۡ وَفِي ٱلرِّقَابِ وَٱلۡغَٰرِمِينَ وَفِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبۡنِ ٱلسَّبِيلِ فَرِيضَةٗ مِّنَ ٱللَّهِ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٞ﴾

Innama alssadaqatu lilfuqara-i waalmasakeeni waalAAamileena AAalayha waalmu-allafati quloobuhum wafee alrriqabi waalgharimeena wafee sabeeli Allahi waibni alssabeeli fareedhatan mina Allahi waAllahu AAaleemun hakeemun*(Surat At Tawbah 9:60)*

Tafsir: ***Hakika ya Sadaka (Zakkah) Nia Kwa Mafukara Na Masikini Na Wanaoisimamia Kuikusanya Na Kuwavutia (Waislam na Wasiokua Waislam) wenye Kuelemezea Nyoyo zao Katika Uislam. Na Kwa Ajili ya Kuwaachisha Huru Watumwa (Mateka n.k) Na Wenye Madeni na Kwa Ajili ya Njia ya* Allah Na Kwa Wasafiri(Waliofikwa na Matatizo ugenini) Huo Ni Wajibu Kutoka kwa Allah Na Allah Ni Mwenye Kujua juu ya Kila kitu na ni Mwingi wa Hikma**

Ambapo aya imetaja aina 8 za Wanaostahiki kupewa Zakkah. Na kwa Upande wa Mujadid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii basi yeye anasema kuhusiana na aya hii: '**Zakkat Hairuhusiki kuwapa wasiokuwemo kwenye Aya Wala Baadhi tu ya Waliotajwa kwenye Aya hii.'***(Hashiyah Al Bajuri aAla Sharh Al Minhaj)*

Imam Sulayman Al Bajuri Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Maimamu watatu wamesema kua Inakubalika Kutumia Zakkah kwa kuwapa watu wa aina mmoja Tu kati 8 ya Hawa**. **Na miongoni mwa wenye Mtizamo huo ni Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kwani anasema kua: Maana ya Aya maneno yasemayo kua Zakkah ni kwa tu ya, Yanamaanisha Kua ni kwa Ajili ya Watu wenye Sifa 8 hizi tu na wala si kwa wengineo, Hivyo hakuna ulazima wa Kuwajumuisha wote kwa kuwapa kwa Pamoja.'***(Hashiya Al Bajuri AAla Sharh Al Minhaj)*

Ambapo kuhusiana na Kiwango ambacho Wanostahiki kupewa watu wenye sifa hizi hawa basi Wanazuoni wametofautiana juu yake. **Kwani kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua: Watu hawa hupewa kile kiasi ambacho kitawatoa kwenye Matatizo yao na kuwahakikishia Usalama wao katika Mahitajio yao ya Muda mrefu wa Maisha yao.'***(Al Majmuu)*

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wanasema kua: **'Watu hawa watapewa kile kitakachowatosheleza kwa Mahitajio yao wao na wale walio chini yao kwa Mda wa Mwaka mmoja wa Mzunguko wa Zakkah.'** *(Hashiyah Al Dasuqi, Al Insaaf)*

Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi Wanasema kua: **'Haikubaliki kuwapa watu hawa zaidi ya Dirham 200, na hivyo kama Mtu anao wanaomtegemea kama Mke na Watoto basi inaruhusika kwa kila mmoja kwa kiwango hicho.'***(Al Muhalla)*

Ambapo tunapoangalia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii ambao ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwetu leo hii kwani ni wanaosema kua Zakkat hua anapewa Mtu ili anyanyuke na yeye Mwakani aweze kutoa Zakkah yaani Umpe Mtu Mtaji Mzima. Wakati hakuna Ulazima huo katika Hili mbali ya kua huo ndio Mtizamo wa Madhha ya Imam Al Shafii na hakuna haja ya Kulaumiana kwa sababu anasema Imam Sulayman Ibn Umar Ibn Mansur Al Ajli Al Jamal Al Yaman Al Shafii kua: '**Kuna Mambo Matatu kuhusiana na Zakkah ambayo Fatwa zake zinatofautiana na Mtizamo wa Skuli ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii, ambayo ni Kuhamisha Zakkat kutoka Mji mmoja kwenda kulipia kwa watu wa Mji mwengine, Kutoa Zakkah kwa kuwapa Watu wa aina Moja tu kati ya aina 8 zilizotajwa kwenye Aya na Kumpa Mtu mmoja tu miongoni mwa Aina Moja kati ya aina 8 za Watu wanaostahiki kupewa Zakkah.'***(Hashiyah Al Jamal Al Ajli)*

Na kwa upande wa Hujjat Ul Islami Mujaddid Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii basi yeye ana Mtizamo kama wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Hanbal kwa kusema kua**: 'Zakkah inatakiwa kumpa Mtu kiasi cha Matumizi ya**

Mzunguko wa Mwaka Mzima wa Zakkah,na hii ni kutokana na asili ya kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alikua ni mwenye kuweka Mipango ya chakula cha Mwaka Mzima kwa ajili ya Familia yake.'

'Na pia kuna mitizamo Tofauti kuhusiana na kiasi gani ambacho Mtu anatakiwa apewe Zakkah, kwani kuna Wanazuoni wasemao kua Hata kiasi ya Chakula cha Siku Moja pia Hutosheleza, huku wakitoa hoja ya kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alipompa Sahl Ibn Hanzala Radhi Allahu Anhu Zakkah na kusema kua Hii ni kwa ajili ya Kumzuia Mtu kuomba Kwa Tajiri, na alipoulizwa 'Utajiri ndio nini?' Akasema ni; 'Chakula cha Mchana na Usiku.'*(Ihya Ulum Ad Din)***

Ambapo anasema Mwalimu wa Imam Ibn Hajar Al Asqalani ambae ni Imam Abu Hafs Siraj Ad Din Al Bulqini Al Shafii kua: Kinachosemwa kuhusiana na Kutokukubalika kuhusiana na kuchanganya Hukmu mbili tofauti ni kwa Ibada Moja, kwa mfano: '**Kama Mtu atatia Udhu kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua kugusana na Mwanamke hakutengui Udhu. Lakini akawa ni mwenye kufuata Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kwa kupaka Maji katika sehemu tu ya Kichwa isiyofikia hata Robo ya Kichwa na kisha akasali basi Sala ya Mtu huyo itakua Batili.**

Na hii ni kwa Sababu Maimamu wote wawili hawa hawatokubali kua Udhu wa Mtu husika Umesihi. **Lakini kwa Upande mwengine kama Ikiwa Mchanganyo husika utakua ni Juu ya ibada mbili tofauti Basi Kuchanganya Mitizamo miwili ya Madhhab tofauti hautopelekea kubatilika kwa Ibada mbili hizo tofauti.**

Yaani kwa Mfano Kama Mtu atafuata Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kuhusiana na Muelekeo wa Kibla katika Kusali kwake, huku katika Kutoa Udhu kwake ametia udhu kama Mfuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii yaani bila Kupaka Maji robo nzima ya Kichwa basi Sala yake Mtu huyo haitobatilika Na hii ni kwa sababu Maimamu Wawili wote hawa hawakukubaliana kuhusiana na Kubatilika kwa Udhu wa Mtu husika kwani kuna Kutokukubaliana juu ya Udhu wake.'*(Tashih Al Minhaj)*

Na akasema Imam Zayn Ad Din Al Malibari kua: '**Mimi nimeona Fatwa ya Al Bulqini kuhusiana na kufanya Talfiq katika Ibada mbili tofauti kua hakubatilishi Ibada.'**(Fat-hu Al Muin)

Kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Al Muhaqqiq Imam Muhammad Ibn Amin Ibn Umar Ibn Abd Al Aziz Ibn Aabidin Al Shaami Al Hanafi kua: '**Kama ikiwa Mtu analiona Ak Kaabah basi anatakiwa aliekee Moja kwa Moja kwa uso na Mwili yaani Ayni Al Qibla**. **Lakini kama hulioni basi unatakiwa uelekee Muelekeo wa Jumla wa Upande wa Al Kaabah yaani Jihat Al Qibla. Ambapo katika muelekeo wa Jihat Al Qibla basi hua hakuna Ulazima wa Mtu kulielekea Moja kwa moja Al Kaabah kwa sababu ya Kuweza kuwepo kwa ugumu wa kukabiliana na Al Kaaba moja kwa moja**.'*(Radd Al Mukhtar)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi anasema Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Naqib Al Misri Al Shafii kua: '**Kuelekea Kibla hua ni Sharti la Kukubalika kwa Sala kwa upande wa Madhhab Ya Imam Al Shafii, isipokua pale itakapokua hakuna uwezekano huo kama Mtu katika wakati wa Kusali kwa mfano Mtu akiwa safarini.**

Hivyo ni Sharti La Sala kuelekea sawasawa katika upande wa Al Kaabah kwa kadri itakavyowezekana katika Madhhab ya Imam Al Shafii.'*(Umdat Salik wa Uddat An Nasik)*

Ambapo kwa upande wa Imam Ibn Rifaah Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Muhammad Al Shafii kua **Kuna Mtizamo wa Imam Al Shafii ambao unasema kua Mtu aliekua mbali na Mji wa Makkah basi anatakiwa aelekee Muelekeo wa Jumla wa Al Kaabah (Jihat Al Kaabah), na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: Baina ya Mashariki na Magharibi kuna Kibla.'*(Imam At Tirmidhi, Imam Ibn Majah)***

Ambapo Mtizamo huu umenukuliwa na Imam Al Muzani, na hivyo kutokana na kua umenukuliaa na Imam Al Muzani basi baadhi wanasema kua Huu ni Mtizamo wa Qawl Al Jadid wa Imam Al Shafii, kwa mfano Imam Abu Hasan Al Juri, muandishi wa Murshid ameupendelea zaid.'*(Kifayat Al Nabih Sharh At Tanbih Fi Fiqh Imam Al Shafii)*

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii basi amesema kua**: 'Huo ndio pia Mtizamo wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu,* Imam Abdullah Ibn Mubarak na Imam Abu Hanifa**.'*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na mtizamo huu ndio pia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal. Hivyo tunapoangalia kuhusiana na Mtizamo wa Muelekeo wa Kibla basi tunaona kua mbali ya Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii umetofautiana na Mtizamo wa Madhhab mengineyo lakini i akubalika kwa mtu aliekua mbali na Al Kaabah kuelekea katika Muelekeo wa Jumla wa Kibla katika Sala kwa sababu tofauti ya Mtizamo wa Udhu na Muelekeo wa Kibla ni Mitizamo ya Vitu viwili tofauti vinavyojitegemea.

Naam baada ya kuangalia mifano kutokana na Mitizamo ya Wanazuoni kuhusiana na Talfiq yaani Kuchanganya Hukumu za Madhhab mawili tofauti katika Ibada Moja na kuona kua hakukubaliki. Lakini hua inakubalika kuchanganya Mitizamo ya Madhhab mawili tofauti katika Ibada mbili au tatu tofauti. Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Al Muhaqqiqin Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Ansari Al Shafii kuhusian na Talfiq kua: **'Mtu anaefuata Mitizamo ya Fiqh ya Skuli za Madhahab tofauti bila ya kua na Dharurah, bali kwa ajili ya kutafuta Urahisi tu katika ufanyaji Ibada basi hua ni mwenye Kufanya Dhambi,na hivyo hua ni Fasiq.'***(Ianat Talibin)*

Fasiq hua ni Mtu mwenye sifa ya kupenda kufanya Maovu na hivyo kua ni mwenye kuvuka mipaka ya Hukumu za Sharia za Dini ya Kiislam na hivyo kua ni mwemye kupotoka kutoka katika Njia iliyo sahih na kuingia kwenye njia ya Upotovu.

Kwani Mtu anaefanya Talfiq bila sababu maalum au dharurah hua ni mwenye kuyakimbia Majukumu ya Dini yake kisharia kutokana na kufuata matamanio ya Nafsi yake.

Hivyo Muislam hua hatakiwi kufanya Talfiq isipokua kwa kufuata njia zilizowekwa wazi na Wanazuoni ambazo hua hazipingani na Malengo ya Sharia za *Allah Subhanah wa Ta'ala* ambayo ni yenye malengo ya Kuhifadhi Imani ya Dini ya Kiislam, Kuhifadhi Uhai, Kuhifadhi Ufahamu, Kuhifadhi Kizazi na Kuhifadhi Mali.

Na bila ya shaka ili mtu usipingane na Malengo hayo basi inabidi kufuata yale ambayo Wanazuoni wameweka wazi kua ni Sahih Na hivyo ni yenye kumuongoza Mhusika katika njia Sahih ya Uongofu. Kwani amesema Imam Abu Daud na Imam At Tirmidhii kua:

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ حَسَّانَ السَّمْتِيُّ، حَدَّثَنَا خَلَفُ بْنُ خَلِيفَةَ، عَنْ أَبِي هَاشِمٍ، عَنِ ابْنِ بُرَيْدَةَ، عَنْ أَبِيهِ، عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَ " الْقُضَاةُ ثَلاَثَةٌ وَاحِدٌ فِي الْجَنَّةِ وَاثْنَانِ فِي النَّارِ فَأَمَّا الَّذِي فِي الْجَنَّةِ فَرَجُلٌ عَرَفَ الْحَقَّ فَقَضَى بِهِ وَرَجُلٌ عَرَفَ الْحَقَّ فَجَارَ فِي الْحُكْمِ فَهُوَ فِي النَّارِ وَرَجُلٌ قَضَى لِلنَّاسِ عَلَى جَهْلٍ فَهُوَ فِي النَّارِ "

Amesema Muhammad Ibn Hasan kua amesema Khalafu Ibn Khalifatan kua amesema Abi Hashim kua amesema Abi Buraydah kua amesema Baba yake kua *amesema Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Mahakim wako wa aina 3: Aina ya Kwanza ni Watu wa Peponi na Aina Mbili ni za Watu wa Motoni. Ama kuhusiana na Wa Peponi basi ni wale ambao ni Wenye Kujua Haki na Wakahukumu kulingana nayo. **Na anaejua haki kisha akahukumu Kinyume chake basi hua ni wa Motoni, na Mwenye kuhuhumumu bila ya kua na Ilm pia hua ni mwenye kuingia Motoni.'** *(Imam At Tirmidhii, Imam Abu Daud na Imam Ibn Majah)*

Hivyo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab mengineyo yote Wanakubaliana kua Tawwaf haisihi bila ya kua na Udhu. Na kutosihi kwa Tawaf hua ni Kwenye Kubatilisha Ibada ya Hija na Umra. Isipokua kwa upande wa Imam Abu Hanifa ambao wao Wanasema kua Udhu hua ni Wajib lakini si Lazima katika Tawwaf.

Kwa maana hio basi kama tukiamua kufuata Mtizamo huu wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi itabidi Tubadilishe Utaratibu na kanuni zote za Ibada ya Hija kutoka kwenye Madhhab ya Imam Al Shafii na kufuata Mtizamo wa Imam Abu Hanifa.

Jambo ambalo linakubalika kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni. Ila sasa tatizo ni kua kuna tofauti takriban 20 baina ya Fiqh ya Ibada ya Hija kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Madhhab ya Imam Abu Hanifa.

Jambo ambalo litazidisha Ugumu kwani itabidi tukifunze Fiqh ya Madhhab ya Imam Abu Hanifa kuhusiana na Ibada nzima ya Hija hatua kwa hatua kwa hivyo tunaachana nayo rai hio.

Rai ya pili ambayo inakubalika pia na Makubaliano ya Wanazuoni ni kupitia Mtizamo wa Uasili wa Udhu yaani kutia Udhu kulingana na Mtizamo wa Fiqh ya Madhhab mengine isiyokua ya Imam Al Shafii na kisha Tufanye Tawwaf kwa kutumia Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo kama tulivyoona kua Madhhab mengine yote yanasema kua Udhu haubatiliki kwa kugusana na Mtu wa Jinsia nyengine isipokua kwa Matamanio.

Lakini kwa upande Fiqh ya wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni kua Udhu unabatilika kwa kugusana na Mtu wa jinsia nyengine ambae unaweza kuoana nae iwe kuhusana huko kwa makusudi au kwa bahati mbaya, kwa matamanio au bila matamanio. Ila rai hii ya kutumia Udhu wa Madhhab nyengine pia ina tatizo, kwa sababu inabidi Mtu ujue Fiqh ya Madhhab husika ili uweze kutia udhu utakaokubalika kulingana na Madhhab unayotaka kufuata katika Udhu.

Kama alivyosema Imam Sulayman Ibn Umar Ibn Mansur Al Ijli Al Jamal Al Yaman Al Shafii ambae amesema kua: '**Moja kati ya Masharti ya Kushikamana na Madhhab mengine hua ni Kutosababisha Talfiq. Talfiq hua ni kuchanganya Mitizamo miwili ya Madhhab na kupata**

Mtizamo mmoja usiokubalika na Dhehebu lelote,kwa mfano:Mtu kutia Udhu na kisha akagusana na Mwanamke bila kua na Matamanio, na hivyo Udhu huo hua ni Sahih kulingana na Madhhab ya Imam Malik.

Lakini sasa tatizo ni kua Katika kutia Udhu kwake Mtu huyo basi hakusugua viungo husika vya udhu, jambo ambalo Kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii ni kua hakuna Ulazima wa kusugua, lakini kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi Kusugua Viungo vya Udhu katika wakati wa kutia Udhu hua ni Sharti la kukubalika Udhu, hivyo kama hukusugua basi Udhu hua ni Batili.

Na hivyo kam akisali Mtu huyo basi Sala yake hua ni batili na hii ni kutokana na Kua Madhhab yote yanakubaliana juu ya kutokubalika Udhu wake kulingana na Mtizamo wa Madhhab haya.' *(Hashiyah Al Jamal)*

Hivyo rai hii ingawa ni rahisi lakini nayo itakua ngumu kwa wengi sana wasiojua tofauti za Udhu katika Madhhab na hivyo haki hii itampelekea mtu kutokua na Udhu kabisa. Na tunajaribu kufafanua mitizamo tofauti ili kuainisha Uzito wa Jambo hili kulingana na Rai tofauti.

Kwani kama tulivyoona kuhusiana na Masharti ya Udhu kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kua Unapopaka Maji Kichwa basi sehemu unayotia Maji isipungue Robo ya Kichwa, na kwa upande wa Imam Ahmad Ibn Hanbal basi ni kua Kichwa kizima kitie maji, na Imam Malikkitie Maji na ukisugue.

Lakini kwa upande wa Imam Al Shafii basi hua ni kupaka sehemu tu ya Kichwa. Na kwa mtu aliezoea Udhu wa Madhhab ya Imam Al Shafii miaka yake yote, itakua vigumu kwake kubadilisha mtizamo n.k.

Kwa maana hio basi tumebakiwa na rai ya Mtizamo mmoja wa mwisho ambayo ni Mtizamo wa kubakia katika Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii. Na kama tunakumbuka basi mwanzoni mwa Mada hii tulianza na Fatwa ya Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Ali Al Shirazi Al Firuzabad Al Shafii katika kitabu Chake cha Al Muhadhdhab Fi Fiqh Al Imam Al Shafii ambacho tulisema kua Ndio Kitabu ambacho Shaykh ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi amekifafanua zaid na kutoakitabu cha Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab.

Na nikasema kua tumeanza na Imam Abu Is-haq Al Shirazi kwa sababu tuta.rudia tena baadae ili kufafanua zaidi, kwani bahari ya Ilm hii ni pana na ina kina kirefu. Na tuliona kua Imam Abu Is-haq Al Shirazi alitoa Mitizamo kadhaa baada ya kuifafanua aya 2 za Udhu na Tayammam ambazo ni Aya ya 43 ya Surat An Nisaa na aya ya 6 ya Surat Al Maidah.

Na tukasema kua Imam Abu Is-haq Al Shirazi amehitimisha aliyoyahitimisha baada ya Kupitia vitabu vya Maimamu wakuu 17 wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii. Hivyo baada ya kuangalia Rai tofauti basi tunarudi kwenye Madhhab yetu ya Asili na kutafuta Ufumbuzi ndani yake kama alivyoelezea Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii.

'Ama kuhusiana na Kugusana na Mwanamke basi hua kunabatilisha Udhu. Ambapo hii hua ni pale Mwanamme anapogusa ngozi ya Mwanammke au Mwanamke anapogusa Ngozi ya Mwanamme bila ya kuwepo kwa kizuizi baina yake. Na Hii ni kutokana na Maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* pale aliposema kua:

﴿أَوْ لَٰمَسْتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُواْ مَآءً فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدًا طَيِّبًا﴾

Aw lamastumu alnnisaa falam tajidoo maan fatayammamoo saAAeedan tayyiban *(Surat An Nisaa 4:43).*

Tafsir: ***Au mnapo (لاَمَسْتُمُالنِّسَآء) wagusa wanawake, lakini ikiwa hamtopata maji basi mtayamam kwa mchanga ulio safi,*** *(Al Muhadhdhab Fi Fiqh Imam Al Shafii - Imam Al*

Ambapo juu ya kuhusiana na Alieguswa basi kuna Mitizamo miwili juu yake. Mtizamo wa Kwanza ni kua Udhu Unabatilika. Na hii ni kwa sababu Ni mguso wa baina ya Mwanamme na Mwanammke ndio unaobatilisha Utohara wa Yule alieguswa. Hivyo Udhu wa Yule alieguswa Hubatilika, kama vile unavyobatilika Udhu kutokana na Kuingiliana Kimwili, kwa yule alieingiliwa pia.

Na pia kuna Mtizamo wa kua Haubatiliki kwa sababu Aisha *Radhi Allahu Anha* Amesema katika Hadith kua: 'Nilimkosa mima *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* nilipoamka Kitandani na hivyo nikanyanyuka na kumtafuta. Na hivyo mkono wangu ukagusa Nyayo yake, na hivyo baada ya Sala akaniuliza Jee Shaytani wako Alikujia?'

Hivyo Kama ikiwa Udhu wa Mtu anaeguswa Unabatilika basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* angekata Sala yake. Na kwa kua Kugusa kunabatilisha Udhu basi Udhu wa yule aliegusa ndio unabatilika na wala sio wa yule alieguswa yaani hii hua sawa na Mtu mwenye Udhu kisha akagusa Sehemu za Siri za Mwenzake.

Na hivyo kama ikiwa Mtu Mwanmme atagusa Nywele au Kucha za Mwanammke basi hautobatilila Udhu wake kwa sababu ya kua hapati hisia za Raha kutokana na kugusa vitu hivyo bali hupata hisia za Raha kutokana na kuagalia tu vitu hivyo. kama Mtu akimgusa yule asieruhusika kumuoa basi kuna Mitizamo miwili juu yake. Ambapo wa kwanza ni kua Udhu Unabatilika na hii ni kulingana na maana ya Aya.

Na Mtizamo wa pili ni kua haubatiliki na hii ni kwa sababu hua hakuna hisia za Matamanio kwa yule asieruhusika kumuoa, hivyo hua ni sawa kwa Mwanamme kugusana na Mwanamme mwenzake au kwa Mwanammke Kugusana na Wanawake mwenzake.

Ama kuhusiana na Mwanamke mdogo asietamanika kwa Mtu husika na Mwanammke Mzee asietamanika na mtu husika basi kuna mitizamo miwili juu yake. Ambapo kulingana na Mtizamo wa Mjumuisho wa Aya basi Udhu hua Unabatilika. Lakini kutokana na upande mwengine wa kutotamanika kwa Mwanamke husika basi hua hakubatilishi Udhu, na hivyo hua ni sawa na Kugusa Nywele.'*(Al Muhadhdhab Fii Fiqh Al Imam Al Shafii)*

Hivyo mmoja kati ya Mitizamo hio ni ulue usemao kua: 'Na pia kuna mtizamo wa Kua Udhu haubatiliki, na hii ni kutokana na Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha.'*

Ambapo kulingana na Skuli ya Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua huu ni Mtizamo usiokua na Nguvu, na pia sio Mtizamo Unaokubalika na Kutegemeaa na Madhhab na hivyo hua ni Mtizamo Dhaifu na usiokua na Nguvu.

Lakini hata hivyo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Inakubalika kwa Mufti Kutoa Fatwa kwa kutumia Mtizamo usiokua na Nguvu katika Madhhab pale inapokua Mtizamo huo ni wenye Kusimamia Maslahi ya Jamii na kutokana na**

kua Kuna Umuhimu unaotakiwa kuzingatiwa, bila ya Mufti husika kuona kua kufanya hivyo ni jambo la kawaida Hususan pale itakapokua Mtizamo Unaokubalika na kutegemewa na Madhhab kua ni wenye Ugumu kutekelezeka.'*(Al Majmuu)*

Na amesema Imam Ibn Ziyad Al Shafii kua: '**Hua hakuna tatizo kutoa fatwa ambayo inapingana na Mtizamo wa Mwisho unaotegemewa na Madhhab katika Madhhab kutokana na Dharurah.'**

Na akasema Ba Sudan kuhusiana na Maneno hayo kua**: 'Ambapo maneno haya yanamaanisha kua inaruhusika Kutoa Fatwa inayopingana na Mtizamo wa Mwisho wa Madhhab kutokana na Dharurah hua inaruhusika na inakubalika kisharia.'***(Maqasid Sanniya ila Mawarid Al Haniyah fi Jamii Fawaid Al Fiqhiyyah)*

Hivyo Inakubalika kwa Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii kutumia Mtizamo Dhaifu wa Madhhab aliyoitoa Imam wa Madhhab ya Imam Al Shafii aliezaliaa miaka 45 baada ya Kufariki Imam Al Shafii.

Na huyu si Imam mwengine yeyote isipokua ni Shaykh Al Madhhab, Imam Al As-hab Al Wujuh Aala Madhhab Imam Al Shafii Imam Abu Al Abbas Ahmad Ibn Umar Ibn Surayj Al Baghdadi Al Shafii maarufu kama Imam Ibn Surayj. Hivyo amesema Imam Ibn Surayj kua: **'Udhu hua haubatiliki kutokana na Kugusana baina ya Mwanamme na Mwanamke Ajnabi pale inapokua Hakuna Matamanio baina yao.'***(Al Majmuu)*

Hivyo Ili Mahujjaj wa Madhhab ya Imam Al Shafii wawe Salama kutokana na Hukmu ya kua na Udhu katika Tawwaf basi inawabidi kushikamana na Fatwa hii ya Imam Ibn Surayj Al Al Shafii.

MUBTILAT SALAT – KUTENGUKA KWA UDHU- KUPOTEZA UFAHAMU

❖❖❖❖

Kwani anasema Hujjat Ul Islami Mujaddid Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammaf Ibn Muhammad Al Ghazali Al Tusi Al Shafii kua: '**Wazimu Huondoa Ufahamu, Kuzimia Huuzidi Nguvu Ufahamu na Usingizi Huufunika Ufahamu.'***(Ihya Ulum Ad Din)*

Na amaesema Al Muhaqqiq, Al Allamah Imam Ibn Abidin Al Shami Al Hanafi kua:
Kupungukiwa na Ufahamu kwa Lugha ya Kiarabu hua kunajulikana kama 'Safa' yaani Upumbavu ambayo hua ni hali ya Kiumbe Ibn Adam kua ni mwenye kufanya mambo ambayo yanaenda Kinyume na Maamrisho ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Mambo hayo hua ni kwa mfano Kutumia Mali kwa Israfu bila ya Malengo Maalum, na hivyo hii hua ni kinyume na Kupoteza Ufahamu wa Akili Kwani Kupoteza Ufahamu wa akili hua ni athari inayomuathiri Ibn Adam na hivyo hua ni mwenye kukosa uwezo wa Kujisimamia Kimaamuzi.

Na mtu mwenye kukosa uwezo wa Kujisimamia kimaamuzi kwa mda mfupi hua na uwezo wa Kurudi katika hali yake ya kawaida, jambo ambalo hua ni tofauti na Mtu mwenye kupungukiwa Ufahamu wa akili, ambae hua anazo akili lakini hazitumii ipasavyo. Hivyo Mwenye kupoteza Ufahamu wa akili hua si mwenye uwezo wa kutofautisha Baina ya Jema na Ovu, kwani Ufahamu wake wa akili hua umefikia katika hali ya kutokua na Uwezo wa kufanya kazi kabisa. **Hali hii huweza kumtokea Ibn Adam kutokana na Maradhi, Sumu, Kupandwa na Shaytani, n.k.'***(Nassamat Al Ashar)*

Na akasema Imam Al Haskafi Al Hanafi kua: **'Kupoteza Akili hua ni Kupoteza Ufaham, au hua ni Kuharibikiwa na Ufahamu.'***(Ifadat Al Anwar)*

Naam tuko katika kukumbushana kuhusiana na aina za Sijda katika Uislam ambamo miongoni mwake Sijda hizo tunakutana na Sijda ya Ibada Ya Sala ya Kiislam, kwani Sijda ndio Kitendo Kinachoitofautisha Muonekano wa Nje wa Sala ya Dini ya Kiislam na Sala za Dini nyenginezo.

Kwani neno Sijda limetokana na neno Sajada lenye kumaanisha Kusujudu, Kuinama mpaka Kichwa kikagusa Chini, Kua katika Hali ya Chini, Kuonesha Unyenyekevu wa Hali ya Juu, Na pia neno Sajada humaanisha Unyenyekevu.

Neno Sajada ndio lililotoa neno Masajidun lenye kumaanisha Masjid au Msikiti au sehemu ya Kufanyia Ibada ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Ukaribu anaoweza kua nao Mja Karibu Na Mola wake hua ni pale anaposujudu, hivyo zidisheni maombi ndani yake mara nyingi sana.'(Sahih Muslim)**

Hivyo kwa kua Sijda humpelekea Mja kua na Ukaribu sana na Muumba wake na Na pia neno Sajada humaanisha Unyenyekevu. Neno Sajada ndio lililotoa neno Masajidun lenye kumaanisha Masjid au Msikiti au sehemu ya Kufanyia Ibada ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ukaribu anaoweza kua nao Mja Karibu Na Mola wake hua ni pale anaposujudu, hivyo zidisheni maombi ndani yake mara nyingi sana.'*(Sahih Muslim)*

Hivyo kwa kua Sijda humpelekea Mja kua na Ukaribu sana na Muumba wake na Na pia neno Sajada humaanisha Unyenyekevu.

Neno Sajada ndio lililotoa neno Masajidun lenye kumaanisha Masjid au Msikiti au sehemu ya Kufanyia Ibada ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Ukaribu anaoweza kua nao Mja Karibu Na Mola wake hua ni pale anaposujudu, hivyo zidisheni maombi ndani yake mara nyingi sana.'***(Sahih Muslim)*

Hivyo kwa kua Sijda humpelekea Mja kua na Ukaribu sana na Muumba wake na Na pia neno Sajada humaanisha Unyenyekevu. Neno Sajada ndio lililotoa neno Masajidun lenye kumaanisha Masjid au Msikiti au sehemu ya Kufanyia Ibada ya Kumuabudu *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Ukaribu anaoweza kua nao Mja Karibu Na Mola wake hua ni pale anaposujudu, hivyo zidisheni maombi ndani yake mara nyingi sana.'*(Sahih Muslim)*

Hivyo kwa kua Sijda humpelekea Mja kua na Ukaribu sana na Muumba wake na Na Malengo ya Ibada ya Sala ni kutukaribisha karihu zaid kwa Mola wetu na ndio maana Ibada ya Sala ikaaa na vitendo vingi vya Sijda kuliko vitendo vyengine vyote ndani yake, basi hatuna budi kukumbushana na kufahamishana juu yake Ibada ya Sala ili tupate kufanikisha Malengo ya Ibada ya Sala.

Na ndio maana wakasema wenye kujua kua Man Sajadah Wajadah - Mwenye Kusujudu Hupata Ila sasa ili Mtu uwe ni mwenye Kupata katika Kusujudu kwako ndani ya Ibada ya Sala yako basi inabidi Ujue Kutekeleza Sijda yako na namna ya Kuisali hio Sala yako, kwani vyenginevyo utakua hupatikitu ndani yake hata Usali kwa mda wa miaka 100. Kwani amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '**Kwa hakika Mtu anaweza akawa anasali kwa**

Mda wa Miaka 60, lakini asikubaliwe hata Sala moja kwa sababu ya Kukamilisha Rukuu, bila kukamilisha Sujud,au kwa kukamilisha Sujud lakini bila kukamilisha Rukuu.'*(Targhib wa Tarhib)*

Ambapo hadith hii inaonesha Umuhimu wa Rukuu na Sujud katika Sala na umuhimu wa kufahamu kila kitujuu ya Ibada ya Sala. Hivyo nasi Alhamd lillah tunaendelea kukumbushana kuhusiana na Ibada ya Sala kulingana na Mitizamo ya Madhhab na Maimamu tofauti.

Na anasema Ubaid Allah Ibn Abd Allah Ibn Utbah kua:

دَخَلْتُ علَى عَائِشَةَ فَقُلتُ: أَلَا تُحَدِّثِينِي عن مَرَضِ رَسولِ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ؟ قَالَتْ: بَلَى، - ثَقُلَ النبيُّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ فَقَالَ: أصَلَّى النَّاسُ؟ قُلْنَا: لَا، هُمْ يَنْتَظِرُونَكَ، قَالَ: ضَعُوا لي مَاءً في المِخْضَبِ. قَالَتْ: فَفَعَلْنَا، فَاغْتَسَلَ، فَذَهَبَ لِيَنُوءَ فَأُغْمِيَ عليه، ثُمَّ أفَاقَ، فَقَالَ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ: أصَلَّى النَّاسُ؟ قُلْنَا: لَا، هُمْ يَنْتَظِرُونَكَ يا رَسولَ اللَّهِ، قَالَ: ضَعُوا لي مَاءً في المِخْضَبِ. قَالَتْ: فَقَعَدَ فَاغْتَسَلَ، ثُمَّ ذَهَبَ لِيَنُوءَ فَأُغْمِيَ عليه، ثُمَّ أفَاقَ، فَقَالَ: أصَلَّى النَّاسُ؟ قُلْنَا: لَا، هُمْ يَنْتَظِرُونَكَ يا رَسولَ اللَّهِ، فَقَالَ: ضَعُوا لي مَاءً في المِخْضَبِ، فَقَعَدَ، فَاغْتَسَلَ، ثُمَّ ذَهَبَ لِيَنُوءَ فَأُغْمِيَ عليه، ثُمَّ أفَاقَ فَقَالَ: أصَلَّى النَّاسُ؟ فَقُلْنَا: لَا، هُمْ يَنْتَظِرُونَكَ يا رَسولَ اللَّهِ، والنَّاسُ عُكُوفٌ في المَسْجِدِ، يَنْتَظِرُونَ النبيَّ عليه السَّلَامُ لِصَلَاةِ العِشَاءِ الآخِرَةِ، فأرْسَلَ النبيُّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ إلى أبِي بَكْرٍ بأَنْ يُصَلِّيَ بالنَّاسِ، فأتَاهُ الرَّسُولُ فَقَالَ: إنَّ رَسولَ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ يَأْمُرُكَ أنْ تُصَلِّيَ بالنَّاسِ، فَقَالَ أبو بَكْرٍ – وكانَ رَجُلًا رَقِيقًا –: يا عُمَرُ صَلِّ بالنَّاسِ، فَقَالَ له عُمَرُ: أنْتَ أحَقُّ بذلكَ، فَصَلَّى أبو بَكْرٍ تِلكَ الأيَّامَ، ثُمَّ إنَّ النبيَّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ وجَدَ مِن نَفْسِهِ خِفَّةً، فَخَرَجَ بيْنَ رَجُلَيْنِ –أحَدُهُما العَبَّاسُ– لِصَلَاةِ الظُّهْرِ وأَبُو بَكْرٍ يُصَلِّي بالنَّاسِ، فَلَمَّا رَآهُ أبو بَكْرٍ ذَهَبَ لِيَتَأَخَّرَ، فأوْمَأَ إلَيْهِ النبيُّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ بأَنْ لا يَتَأَخَّرَ، قَالَ: أجْلِسَانِي إلى جَنْبِهِ، فأجْلَسَاهُ إلى جَنْبِ أبِي بَكْرٍ، قَالَ: فَجَعَلَ أبو بَكْرٍ يُصَلِّي وهو يَأْتَمُّ بصَلَاةِ النبيِّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ، والنَّاسُ بصَلَاةِ أبِي بَكْرٍ، والنبيُّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ قَاعِدٌ، قَالَ عُبَيْدُ اللَّهِ: فَدَخَلْتُ علَى عبدِ اللَّهِ بنِ عَبَّاسٍ فَقُلتُ له: ألَا أعْرِضُ عَلَيْكَ ما حَدَّثَتْنِي عَائِشَةُ عن مَرَضِ النبيِّ صَلَّى اللهُ عليه وسلَّمَ؟ قَالَ: هَاتِ، فَعَرَضْتُ عليه حَدِيثَهَا، فَما أنْكَرَ منه شيئًا غيرَ أنَّه قَالَ: أسَمَّتْ لكَ الرَّجُلَ الذي كانَ مع العَبَّاسِ؟ قُلتُ: لَا، قَالَ: هو عَلِيُّ بنُ أبِي طَالِبٍ رَضِيَ اللَّهُ عنْه.

Nilingia Nyumbani kwa Aisha *Radhi Allahu Anha* na kumwambia: 'Hivi Jee utaniambia kuhusiana na Maradhi ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam?'*

Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema : 'Naam, *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akiumwa, na hivyo akauliza: Jee Watu wameshasali?' Nasi tukasema : 'La, bado kwani Wanakisubiri wewe.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Tafadhali nitilie Maji kwenye Beseni kwa ajili yangu.'**

Hivyo Tukamletea Maji na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatia Udhu, Kisha akataka kunyanyuka akajisaidie, lakini akazimia. Kisha akapata Fahamu na kuuliza: 'Jee Watu wameshasali?'

Hivyo nasi tukasema, 'La bado Wanakusubiri wewe *Ya Rasul Allah!(Salallahu Alayhi wa Salam)'*

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Niwekeeni Maji kwenye Beseni kwa ajili yangu.'

Na kisha akakaa kitako na Kutia Udhu, na kisha akaenda Kujisaidia lakini akazimia tena. Kisha akapata fahamu tena na Kuuliza:' Jee Watu wameshasali?'

Hivyo nasi tukasema; 'La, Kwani wanakusubiri wewe ya *Rasul Allah (Salallahu Alayhi wa Salam).'*

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Basi Niwekeeni Maji kwenye Beseni kwa ajili yangu.'**

Kisha akatia Udhu na kuelekea Msalani lakini akazimia, kisha akapata Fahamu tena na Kuuliza: 'Jee watu wameshasali?' Nasi tukasema 'La, kwani Wanakusubiri wewe *Ya Rasul Allah(Salallahu Alayhi wa Salam)'*

Na watu walikua wamekaa Msikitini wakimsubiri *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa ajili ya Kusali Sala ya Al Isha.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatuma aambiwe Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kua Awasalishe watu, na alietumwa akaenda na kumwambia Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anakuamrisha Uwasalishe watu.

Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua Mtu mnyenyekevuna mpole akasema kumwambia Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Umar! Waongoze watu katika Sala.'

Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema: La, kwani wewe Abu Bakr ndie unaestahiki zaidi kusalisha Na hivyo Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* akasalisha katika siku hizo, *ambazo Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akihisi kizunguzungu hivyo alikua akipelekwa Msikitini baina ya Watu wawili na mmoja wao ni Al Abbas *Radhi Allahu Anhu* katika Sala ya Adhuhuri, na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alikua akisalisha.

Na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* alipokua akimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi alikua akijaribu kurudi nyuma, lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua akimuashiria kuendelea Kusalisha na kusema Niwekeni nikae kitako pembeni yake.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akawa anawekwa karibu ya Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu,* na Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu* husalisha huku akiwa anaifuata Sala ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Na watu wakawa wanaifuata Sala ya Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu,* huku *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwa amekaa Kitako.

Ubaid Allah anasema kua: Mimi nikatoka kwa Aisha *Radhi Allahu Anha* na kuelekea kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* na kumwambia: 'Jee nikuambie kile ambacho akichoniambia Aisha *Radhi Allahu Anha* kuhusiana na Kuumwa kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*?'

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Naam, niambie.'

'Nami nikamuelezea kila kitu, na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* hakukanusha kitu chochote isipokua akiniuliza: 'Jee alikuelezea kuhusiana na Mtu wa pili aliekua na Al Abbas *Radhi Allahu Anhu*?'

Nami nikasema 'La!'

Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'Mtu wa pili alikua ni Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu*.'*(Sahih Bukhari)*

Naam..hadith hii ni moja kati ya hadith ambazo zinatuainishia Hukmu zifuatazo:

1-Mtu anapopoteza Fahamu basi Udhu wake hua unatenguka. Na ndio maana *Rasul Allah Salallah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alizimia Mara 4 katika kipindi cha mwishoni mwa uhai wake basi alikua alipokua anapopata Fahamu anatia Udhu tena upya.

2-Inaruhusika kwa Imam asieweza Kusalisha, kwa dharurah Kuwasalisha wale Wanaoweza kusalisha.

3-Inaruhusika kwa Mtu mwenye kua nyuma ya Imam kutoa Sauti ya Hatua za Sala ili kuwataarifu Maamuma kutokana na Dharurah.

4-Mtu anaenadia Hatua za Imam anatakiwa awe aliekaa upande wa Kulia mwa Imamu, aidha ndani ya Safu au mbele ya Safu nyuma ya Imam kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikaa kitako kushoto ya Abu Bakr *Radhi Allahu Anhu.*

5-Inaruhusika Kwa Mtu kubadilisha Nia ya Sala wakati ukiwa ndani ya Sala,kwa mfano kutoka Imam kua Maamuma au Maamuma kua Imam kulingana na Dharurah husika.

Na amesema pia Zir Ibn Hubaysh kua:

عَنْ زِرِّ بْنِ حُبَيْشٍ، قَالَ: أَتَيْتُ صَفْوَانَ بْنَ عَسَّالٍ – رَضِيَ اللهُ عَنْهُ – أَسْأَلُهُ عَنِ الْمَسْحِ عَلَى الْخُفَّيْنِ، فَقَالَ: مَا جَاءَ بِكَ يَا زِرُّ؟ فَقُلْتُ: ابتِغَاءَ الْعِلْمِ، فَقَالَ: إِنَّ الْمَلَائِكَةَ تَضَعُ أَجْنِحَتَهَا لِطَالِبِ العِلْمِ رِضًا بِمَا يطْلُبُ، فقلتُ: إِنَّهُ قَدْ حَكَّ فِي صَدْرِي الْمَسْحُ عَلَى الْخُفَّيْنِ بَعْدَ الغَائِطِ والْبَولِ، وَكُنْتَ امْرَأً مِنْ

أَصْحَابِ النَّبِيِّ –صلى الله عليه وسلم– فَجئتُ أَسْأَلُكَ هَلْ سَمِعْتَهُ يَذكُرُ في ذلِكَ شَيئًا؟ قَالَ: نَعَمْ، كَانَ يَأْمُرُنا إِذَا كُنَّا سَفْرًا – أَوْ مُسَافِرِينَ – أَنْ لَا نَنْزِعَ خِفَافَنَا ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ وَلَيالِيهنَّ إِلَّا مِنْ جَنَابَةٍ، لكنْ مِنْ غَائطٍ وَبَولٍ ونَوْمٍ، فقُلْتُ: هَلْ سَمِعْتَهُ يَذْكُرُ فِي الْهَوَى شَيْئًا؟ قَالَ: نَعَمْ، كُنّا مَعَ رسولِ اللهِ –صلى الله عليه وسلم– في سَفَرٍ، فبَيْنَا نَحْنُ عِندَهُ إِذْ نَادَاهُ أَعْرَابِيٌّ بصَوْتٍ لَهُ جَهْوَرِيٍّ: يَا مُحَمَّدُ، فأجابهُ رَسُولُ اللهِ –صلى الله عليه وسلم– نَحْوًا مِنْ صَوْتِه: «هَاؤُمْ» فقُلْتُ لَهُ: وَيْحَكَ! اغْضُضْ مِنْ صَوتِكَ؛ فَإِنَّكَ عِنْدَ النَّبي –صلى الله عليه وسلم– وَقَدْ نُهِيتَ عَنْ هذَا! فَقَالَ: وَاللهِ لَا أغْضُضُ، قَالَ الْأَعْرَابِيُّ: الْمَرْءُ يُحِبُّ القَوْمَ وَلَمَّا يَلْحَقْ بِهِمْ؟ قَالَ النَّبِيُّ –صلى الله عليه وسلم–: «المرْءُ مَعَ مَنْ أَحَبَّ يَومَ القِيَامَةِ»، فَمَا زَالَ يُحَدِّثُنَا حَتَّى ذَكَرَ بَابًا مِنَ المغْرِبِ مَسيرَةُ عَرْضِهِ أَوْ يَسِيرُ الرَّاكبُ في عَرْضِهِ أَرْبَعينَ أَوْ سَبعينَ عامًا – قَالَ سُفْيانُ، أَحدُ الرُّواةِ: قِبَلَ الشَّامِ – خَلَقَهُ اللهُ تَعَالَى يَوْمَ خَلَقَ السَّمَاواتِ والْأَرْضَ مَفْتُوحًا «رواه الترمذي، وغيره، وقال: «حديث حسن صحيح للتَّوْبَةِ، لَا يُغْلَقُ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ مِنْهُ،

Nilienda mimi kwa Safwan Ibn Asal *Radhi Allahu Anhu* kumuuliza kuhusiana na Kupangusa juu ya Soksi nyepesi za Ngozi katika Udhu, na akaniuliza: 'Ni Kitu gani kichokuleta hapa ewe Zirr?'

Nami nikajibu : 'Nimekuja Kutafuta Ilm'

Ambapo nae akasema: 'Hakika ya Malaika hua ni wenye Kuteremsha Mabawa yao kwa ajili ya Watafutao Ilm Kutokana na Furaha yao Malaika ju ya Mtu mwenye kutafuta Ilm.'

Nami nikasema: 'Mimi nina shaka juu ya Kupangusa juu ya Soksi za Ngozi katika wakati wa Kutia Udhu baada ya Kujisaidia haja ndogo na haja kubwa. Na kwa kua wewe ni mmoja kati ya Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* basi nimekuja kukuuliza kama umewahi kusikia chochote kuhusiana na Jambo hili.'

Safwan Ibn Asal *Radhi Allahu Anhu* akajibu kwa kukubalia na kisha akasema: *'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituelekeza sisi katika wakati tunapokua Safarini, kua haina haja ya Kuvua Soksi Nyepesi za Ngozi hadi kwa mda wa siku tatu usiku na Mchana,isipokua pale tutakapokua na Janaba. Lakini katika hali nyengine kama Kulala usingizi, Kujisaidia haja Ndogo na Kubwa basi hua inatosheleza kupanguza tu juu ya Soksi katika Kutia Udhu.'

Zirr anaendelea kusema kua: 'Mimi nikamuuliza Safwan Ibn Asal *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema: Jee umemsikia wewe *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema chochote kuhusiana na Mapenzi?'

Ambapo nae akajibu: 'Naam, wakati tuilipokua Safarini na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* alitokea Bedui ambae alimwita *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa sauti kubwa sana Kwa kusema : Ya Muhammad!'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akaitikia kwa sauti ya kubwa pia kwa kusema: 'Niko Hapa!'**

Safwan Ibn Asal *Radhi Allahu Anhu* anasema: 'Hivyo mimi nikamwambia Bedui huyo kua: Shusha chini Sauti yako kwani Upo mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na huruhusiki kupaza Sauti!'

Bedui huyo akajibu: 'Wa Allahi sitoshusha Sauti yangu!'

Kisha akasema kwa kunadia kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam:* 'Jee unasemaje kuhusiana na Mtu anaewapenda watu lakini akawa hawezi kukutana nao?'

Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam **akasema: 'Kila Mtu atakua pamoja na Wale anaowapenda katika siku ya Malipo.'**

'Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akaendelea kutuambia sisi na katika kusema kwake akataja Mlango katika maeneo ya Magharibi ambao upana wake ni sawa na Masafa ya safari ya Miaka 40 au 70 ya mpanda Farasi.'**

Ambapo mmoja kati ya Walionukuu Hadith hii aitwae Sufyan amesema kua: 'Mlango huo uko katika Muelekeo wa Sham na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameuumba tangu siku aliyoumba Mbingu na Ardhi na Mlango huo uko wazi kwa ajili ya Kutubu na hautofungwa hadi pale Jua litakapochomoza kutoka katika Upande huo.'*(Hasan Hadith,Imam Ibn Majah, Imam At Tirmidhii na Imam Ahmad Ibn Hanbal)*

Kwani hii pia ni Hadith inayothibitisha kua Kupoteza faham, Kulala hua kunabatilisha Udhu na ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamrisha Masahaba zake *Radhi Allahu Anhu* kua Watakapolala basi wakiamka itawabidi watie Udhu, na kwa kua wako Safarini basi wataruhusika kupangusa Khuf (Soksi za Ngozi Laini) zao kama kkiwa hawana Janaba, kwani ikiwa wana Janaba baso itawabidi wazivue kisha wakoge au watayammam.

Na ingawa hadith hii imebeba ujumbe tofauti ndani yake wenye manufaa lakini mara nyingi Wengi hua wananukuu sehemu tu ya Hadith kulingana na Mada, ila mimi kwa kua si mwenye kujua basi hua napenda kunukuu Hadith nzima kwa sababu ya kunufaisha wengine miongoni mwa wenzangu wasiojua yale mengineyo yaliyomo kwenye Hadith husika ambayo ni Pamoja na:

1-Umuhimu wa Kutafuta Ilm na Kuuliza wale wanaojua juu ya yale tusiyoyajua.

2-Uhalali wa kupaka juu ya soksi, muda wake ambao ni siku tatu mchana na usiku kwa msafiri, na siku moja na usiku mmoja kwa mkazi.

3-Kupangusa juu ya soksi hua kunaruhusiwa tu katika hali za Najis ndogo.

4-Ruhusa ya kumuuliza muulizaji kuhusu ushahidi wa mwanachuoni, iwe ni matini, ushahidi usio na shaka, au ijtihadi yake binafsi. Msomi hatakiwi kuona haya.

5-Kuwa na adabu na Wanazuoni na watu wema, na kuteremsha sauti katika mikusanyiko ya Wanazuoni.

6-Kuwafundisha wajinga tabia njema na kanuni za mwenendo.

7-Kuiga mfano wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika ustahimilivu wake, tabia yake njema, na kuwahutubia watu kulingana na kiwango cha elimu na akili zao.

8-Kuwa na hamu ya kukaa na watu waadilifu, kuwa karibu nao, na kuwapenda.

9-Upendo humvuta mpenzi kwenye njia ya yule anayempenda na kumtia moyo kumtii anaependa

10-Hufungua mlango wa matumaini na matarajio, huleta habari njema za wokovu, na ni mpole katika mawaidha.

11-Ukubwa wa rehema za Mwenyezi Mungu, Mwenyezi, na kufungua kwake mlango wa toba.

12-Kuwasihi watu waharakishe kutubu, wajiwajibishe wenyewe, na wamrudie Mungu Mwenyezi.

Na amesema Muawwiyah Ibn Abi Sufyan kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

إنَّما العينُ وِكاءُ السَّهِ فإذا نامت العينُ انطلق الوِكاءُ فمَن نامَ فليتوضَّأ

Hakika ya Jicho ni Kizuizi cha Kamba ya Upinde, Hivyo Jicho Linapofumba Basi Kizuizi Huachia, Hivyo yeyote yule atakaelala, na Atie Udhu.'

Na pia kuna hadith isemayo:

حدثنا بقية عن الوضين بن عطاء عن محفوظ بن علقمة عن عبد الرحمن بن عائذ عن علي بن أبي طالب رضي الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: وكاء السه العينان فمن نام فليتوضأ

Amesema Ataa akua amesema Mahfudh Ibn Al Kamah kua amesema Abd Rahman Ibn Aaidh kuaa amesema Ali Ibn Abi Talib Radhi Allahu Anhu kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kizuizi cha Upinde wa Macho Mawili, hivyo atakaelala basi na Atawadhe' *(Imam Ibn Mulaqqin katika Badr Al Munir, Imam At Tabrani, Imam Ahmad, Imam Al Bayhaqi, Bulugh Al Marami, Sunnan Abu Daud)*

Naam anasema Imam Abi Abd Rahman Sharrafi Al Haqq Muhammad Ashraf Sadiq Al Adhiim Al Aabadii katika Kitabu chake cha Awn Al Maabudi Sharh Sunnan Abi Daud kuhusiana na Hadith hii kua: '**Anasema Imam anasema Al Hafidh, Al Lughawi, Al Aalamah Imam Abu Sulayman Hamd Ibn Muhammad Al Khattabi Al Busti Al Shafii Kua:**

Al Ssah hua ni Sehemu ya Siri ya Haja Kubwa, na pia humaanisha Kitanzi Kinachotumiwa Kufunga Mdomo wa Kibuyu cha Ngozi Cha Maji na Vitu kama hivyo, ambapo kuna msemo wa kiarabu usemao kua Ihfadh Ma Fii Alwiyaa Bishadi Al Waka - Kihifadhi Kilichomo Ndani ya Chombo kwa kukaza Kitanzi, na hivyo humaanisha pia Kua Macho hua Kunadhibiti sehemu za Siri za Haja Kubwa,na Hivyo huzuia kila kinachotaka kutoka Ndani yake mtu kwani Mtu akiwa Macho hua ni mwenye Kuhisi kile kinachotaka Kumtoka.'*(Awn Al Muabud Ala Sharh Sunna Abu Daud)*

Na amesema Al Hafidh Imam Izz Ad Din Abu Al Hasan Ali Ibn Muhammad Ash Shaybani Ibn Al Athir Al Shafii kua: 'Maana yake hadith hii ni kua Mtu aliekua Macho hua ni sawa na Mtu ambae Sehemu zake za Siri zimezibwa kwa Kitambaa lakini anapolala huregea Kitanzi chake. Na Imam Al Tibbi amesema kua: Mtu anapokua yumacho basi hus ni mwenye kuweza kuzia kilichomo Tumboni mwake lakini anapolala basi hupoteza hiari yake na Misuli huachia.' *(Awn Al Muabud Ala Sharh Sunna Abu Daud)*

Naam..hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametumia Lugha ya Kumithilisha katika hadith hizi ambazo ndani yake mna hukmu inayotuonesha kua Kulala Usingizi hakutengui Udhu bali hua ni sababu inayopelekea kutenguka kwa Udhu pale inapokua Usingizi huo ni Mzito sana kiasi ya kua Mtu husika kufikia kupoteza fahamu na kutojifahamu juu ya kile kitakachotokea ndani ya Mwili wake wakati akiwa Usingizini, kwani hua ni sawa na aliezimia na hata alielewa pia.

Kwani mbali ya kuwepo kwa hadith tulizoziangalia kuhusiana na Kulala na kupoteza fahamu na kubatilika kwa udhu lakini hata hivyo Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Usingizi na Kubatilika kwa Udhu,kwani kuna wasemao kua:

1-Usingizi haubatiliahi Udhu kabisa na hii ni kutokana na Uthibitisho wa Haditj ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua wakimsubiri *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua wakisubiri Sala ya mwisho ya Al Ishaa hadi Vichwa vyao hugongana, na kisha husali bila kutia Udhu, hivyo hii inathibitisha kua Usingizi haubatilishi Udhu kwani kama ingekua unabatilisha basi isingeruhusiwa hivyo na *Allah Subhanah wa Ta'ala* angemjuulisha *Rasul Allah Salalahu Alayhi wa Salam* juu ya hilo.

2-Usingizi Unabatilisha Udhu iwe Kidogo au Mwingi, na hii ni kutokana na Hadith ya Safaan Ibn Assal Ambae amesema kua sisi tukiiua tukisafiri na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* nae akatuamrisha Kupangusa kwenye Soksi zetu za Ngozi kama tukizivaa huku tukiwa tohara, kwa mda wa siku 3 usiku na mchana tukiwa safarini.

Na kwa siku Moja Usiku na Mchana tukiwa hatuko safarini, na tusizivue katika wakati wa Kujisaidia haja jubwa, haja ndogo au Kulala, iipokua kama tukiwa na Janaba.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameainisha Najis Zitakazopelekea kutovuliwa kwa Soksi ambapo ndani yake amejumuisha Usingizi, na hivyo kumaanisha kua Usingizi unabatilisha Udhu, hususan baada ya kuujumhisha na Haja ndogo na Kubwa, ambazo zote hubatilisha Udhu kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni.

Hivyo Usingizi umefanywa kua ni wenye kubatilisha Udhu kama Haja ndogo na kubwa kama ilivyosemaa kwenyw Hadith ya Aki Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Yeyote yule atakaelala basi na atie Udhu Zitakazopelekea kutovuliwa kwa Soksi ambapo ndani yake amejumuisha Usingizi, na hivyo kumaanisha kua Usingizi unabatilisha Udhu,hususan baada ya kuujumhisha na Haja ndogo na Kubwa, ambazo zote hubatilisha Udhu kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni.

Hivyo Usingizi umefanywa kua ni wenye kubatilisha Udhu kama Haja ndogo na kubwa kama ilivyosemwa kwenye Hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Yeyote yule atakaelala basi na atie Udhu Zitakazopelekea kutovuliwa kwa Soksi ambapo ndani yake amejumuisha Usingizi, na hivyo kumaanisha kua Usingizi unabatilisha Udhu, hususan baada ya kuijumuisha

na Haja ndogo na Kubwa, ambazo zote hubatilisha Udhu kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni.'

Hivyo Usingizi umefanywa kua ni wenye kubatilisha Udhu kama Haja ndogo na kubwa kama ilivyosemwa kwenye Hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Yeyote yule atakaelala basi na atie Udhu zitakazopelekea kutovuliwa kwa Soksi ambapo ndani yake amejumuisha Usingizi, na hivyo kumaanisha kua Usingizi unabatilisha Udhu,hususan baada ya kuujumhisha na Haja ndogo na Kubwa, ambazo zote hubatilisha Udhu. Na hadith hii haikutofautisha baina ya Kulala kidogo na Kulala fofofo.

3-Usingizi Mzito ndio hubatilisha Udhu, lakini kulala kidogo tu hakubatilishi Udhu'

4- Kama ikiwa Mtu atapatwa na Usingizi katika moja kati ya hatua za Sala, kwa Mfano katika Kuruku, Kusujudu, Kusimama au Kukaa basi Udhu wake hautibatilika, iwe mtu huyo yumo ndani ya Sala ama la.

Ila kama ikiwa atalala huku akiwa amelala chini, au amelalia mgongo basi Udhu wake utabatilika. Ambapo huu ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Dhahiri na pia kuna Kauli moja ya upekèe katika Madhhab ya Imam Al Shafii kama alivyosema Imam An Nawawi

Na Uthibitisho wao ni kutokana na Hadith ya Malik kutoka kwa Umar *Radhi Allahu Anhu* ambayo Sanad yake imekatika isemayo kua: 'Kama mmoja kati yenu akilala Usingizi chini basi na atie Udhu.'

Na kuna Hadith kutoka kwa Imam Bayhaqi ambao Sanad yake imekatika pia isemayo kua: Amesema Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu kua: 'Hakuna Udhu kwa Yule atakae lala huku amepandiaha Mguu wake juu ya mguu mwengine, au alielala huku Akiwa amesimama au alielala huku akiwa katika Sijda hadi atakapolala chini.' Wanazuoni wenye Mtizamo huu wana vithibitisho vya Hadith nyengine pia.

5-Mtizamo usemao kua katika Usingizi kinachobatilisha Udhu isipokua kwa yule alielala huku akiwa kwenye Rukuu au Sijda. Mtizamo huu umenukuliwa kutoka kwa Ahmad Ibn Hanbal, na Imam An Nawawi na hii ni kwa sababu Rukuu na Sujud hubatilika kutokana na Usingizi.

6-Mtizamo usemao kua Usingizi haubatilishi Sala isipokua ksa yule ambae anarukuu au anaesujudu, na hii ni kutokana na Uthibitisho wa Hadith iliyonukuliaa na Imam Ahmad ibn Hanbal katika Al Zuhd isemayo kua: 'Wakati Mja anapokua amelala huku akiwa katika Sijda, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* husema: Mwangalieni Mja wangu, Roho yake iko pamoja Nami wakati akiaa katika Sujud.'

Na wenye Mtizamo huu Wanasema kua hadith hii ni Makhsusi kwa Sujud tu, ingawa inaweza kujumuiahwa na Rukuu.

7-Mtizamo usemao kua Usingizi haubatikishi Salam isipokua Katika Sujud, ambapo Mtizamo huu pia umenukuliwa kutoka kwa Imama Ahmad Ibn Hanbal na Imam An Nawawi. Na hii ni kwa sababu Udhu huweza kubatilika kirahisi zaidi katika Sujud kuliko katika Rukuu.

8-Mtizamo usemao kua Usingizi ndani ya Sala hua hautengui Udhu wala Sala, bali hua unatengui Udhu nje ya Sala. Mtizamo huu umenukuliwa kutoka kwa Imam Al Shafii ambae amesema ni mtizamo wa Imam Abu Hanifa, na ni dhaifu.

9-Mtizamo usemao kua: Kama Mtu ikiwa atakua amepata usingizi huku makalio yake yamekandamizika kwenye Ardhi, basi Udhu wake hautobatilika lakini akiwa amelala katika hali nyengine basi utakua umebatikika.

Iwe mtu huyo amelala kaa mda mfupi tu au kwa mda mrefu, iwe yuko ndani ya Sala ama la, ambapo huu ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo anasema Imam Al Shafii kua Usingizi wenyewe hua si Najis bali hua ni Abu Hanifa, na ni dhaifu 9-Mtizamo usemao kua: Kama Mtu ikiwa atakua amepata usingizi huku makalio yake yamekandamizika kwenye Ardhi, basi Udhu wake hautobatilika lakini akiwa amelala katika hali nyengine basi utakua umebatikika. Iwe mtu huyo amelala kaa mda mfupi tu au kwa mda mrefu, iwe yuko ndani ya Sala ama la. Ambapo huu ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo anasema Imam Al Shafii kua Usingizi wenyewe hua si Najis bali hua ni Uthibitisho wa uwezekano wa Kutokwa na Gesi, na hivyo Shariah inalichukulia jambo hili kua ni la Uhakika. Lakini kama ikiwa makalio yamegamdamizika ardhini basi hua hakuna uwezekano wa kutokwa na gesi, na hivyo Kikanuni hua ni kua Udhu haujabatilika. Ambapo Imam An Nawawi amesema kua: Uthibitisho ni Hadith za Ali, Ibn Abbas na Muawwiyah *Radhi Allahu Anhum.*

Ambapo amesema Al Shawqani kua: 'Huu ndio Mtizamo ninaoukubali zaidi mimi na hii ni kwa Sababu vithibitisho vyake vinaendana sambamba na kukubaliana.'

Ambapo Amir Al Yamani amesema katika *Subula Salaam* kua: 'Baada ya kuchunguza kwa makini kila kithibitisho basi nimehitimisha kua Usingizi mzito ambao utamtoa mtu akili humbatilishia Mtu Udhu iwe Mtu huyo amelala kifudifudi au chali.'

Ama kuhusiana na Mtu atakaelala huku akiwa katika moja kati ya Hatua za Sala basi Udhu wake haubatiliki, iwe yuko ndani ya Sala au nje ya Sala. Na pia Usingizi wa Mtu alielala chini bila kupitiwa na usingizi mzito basi Udhu wake habatiliki, wa Allahu Aalam*(Awn Maabud Fii Sharh Sunnan Abu Daud)*

Naam hizo ni aina 9 za Mitizamo juu ya Udhu na Usingizi kutoka katika kitabu Imam Aabi Abd Rahman Sharafi Al Haqq Muhamad Ashrafi Sadiq.

Naam,anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii katika Kitabu chake cha Al Majmuu Ala Sharh Al Muhadhdhab kua: '**Ama kuhusiana na Usingizi hua inabidi kuangaliwa hali yake, kwani Kama ikiwa Usingizi umemjia mtu wakati akiwa Amelala, Ananing'inia au Ameegemea Kitu basi Udhu wa Mtu husika utabatilika na hii ni kulingana na Hadith ya Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu* ambayo amesema kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Macho ni Kivutio cha Upinde, hivyo kama Mtu akilala basi na Atie Udhu.'**

Na hata ikiwa Mtu atapatwa na Usingizi huku akiwa amekaa Kitako na Makalio yake yamekandamizana na Ardhi, basi anasema juu ya hili Imam Al Buwayti Al Shafii kua Udhu wa Mtu husika utabatilika, ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Al Muzani Al Shafii kulingana na Hadith ya Ali. Na hii ni kwa sababu Kile kinachobatilisha Udhu wakati Mtu akiwa Amelala Ardhini hua pia ni chenye kubatilisha Udhu wakati wa Kukaa.

Ambapo kile kilichozungumziwa katika Vitabu kuhusiana na Kutobatilika kwa Udhu kutokana na Usingizi basi hua ni kulingana na Hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: 'Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* walikua wakisubiri Sala ya Isha, na hivyo walikua Wakilala huku wakiwa wamekaa 'Kitako, na kisha Husali bila Kutia Udhu upya.

Ambapo Amr Ibn Shuayb amesema kua amesema Baba yake kua amesema Babu yake kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaelala Usingizi huku akiwa amekaa Kitako basi haitohitajika kwake kutia Udhu upya, ama yule atakaelalia Ubavu akiwa Usingizini basi hua ni Wajibu wake kutia Udhu.

Ambapo hii ni kinyume na Najis ambayo hua inabatilisha Udhu yenyewe kama Najis, Wakati Usingizi Hubatilisha Udhu kwa sababu ya kua ni wenye kuweza kupelekea kutokwa na Najis bila kuhisi wakati mtu anapogeuka kutoka hali moja kuingia katika hali nyengine, lakini kama ikiwa mtu atakua amekaa kitako basi atakua anahisi Mtoko wa Najis katika Kuka kwake.

Ama kama ikiwa Mtu atapitiwa na Usingizi wakati akiwa anarukuu, au anasujudu au amesimama ndani ya Sala,basi hu kuna Mitizamo miwili juu yake. Ambapo Kulingana na Mtizamo wa Kauli Mpya ya (Qawl Al Jadid) Madhhab ya Imam Al Shafii basi ni Kua Udhu utabatilika, na hii ni kutokana na Hadith ya Ali *Radhi Allahu Anhu* na kwa sababu ya kua Amelaa wakati akiwa si katika hali ya kukaa kitako, hivyo hua ni sawa na alielala wakati akiwa amelala chini.

Ambapo Kulingana na Mtizamo wa zamani *(Qawl Al Qadim)* ya Madhab ya Imam Al Shafii basi ni kua Udhu haujabatilika. Na hii ni kutokana na Kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua 'Kama Mja atalala katika Sala yake, basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* hujisifia kwa Malaika wake kwa kusema: Roho ya Mja wangu iko kwangu wakati Mwili wake ukiwa Umesujudu mbele yangu.' *(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Naam..tunaona kua Wanazuoni wanazungumzia kuhusiana na Mitizamo ya Usingizi ndani ya Sala, ambapo baadhi wanaweza kujiuliza kuhusiana na hali hii, kua inakuaje Mtu alale kwenye Sala?

Ambapo haya ni mambo ambayo yanatokea na hivyo Wanazuoni wanayazungumzia kutufahamisha hukuki zake kwa sababu kuna baadhi ya Watu hua wanapatwa na Usingizi ndani ya Sala, kutokana na Kua Maamuma anasali Nyuma ya Imam ambae kwa mfano anasoma Kisomo cha Sura ndefu ambayo Maamuma haijui labda, au Maamuma amechoka, au Imam anasoma Dhikr Nyingi, au kwa mfano labda katika Sala Al Qiyam Al Layl katika siku za Mikesha Miskitini n.k

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kutuambia kua '**Ama kuhusiana na Mukhtasari wa Mitizamo ya Hukmu kuhusiana na Kulala basi kuna Kauli tano zilizonukuliwa kutoka kwa Imam Al Shafii**. **Na Mtizamo Sahih katika Madhhab ya Imam Al Shafii, na katika Vitabu vyake na Nukuu za Wanafunzi na Wafuasi wake kulingana na Vithibitisho basi ni ule: Usemao kua: Kama Mtu akilala usingizi huku akiwa amekalisha Makalio yake kitako Ardhini, basi Udhu wake hautobatilika.'**

Na hivyo kama Mtu haitowezekana kua ni mwenye kulala hivyo basi Udhu wake utabatilika tu iwe hayuko ndani ya Sala au yuko ndani ya Sala.

Mtizamo wa Pili ni kua Udhu utabatilika kwa vyovyote vile atakavyolala,na hii ni kulingana na Mtizamo wa Imam Al Buwayti.

Mtizamo wa Tatu ni kua kama Mtu atalala ndani ya Sala basi Udhu wake Hautobatilika hata iwe amelala vipi. Na kama ikiwa amelala kwenye sehemu nyengine nje ya Sala bila uwezekano wa kukaa basi Udhu wake utabatilika, lakini kama ikiwa amekaa Kitako basi hautobatilika.

Mtizamo wa Nne Kama ikiwa Mtu atalala katika hali ya kua katika mkao wa Moja kati ya Mikao ya Hatua za Sala basi Udhu hautotenguka, iwe mtu huyo yuko ndani ya Sala au nje ya Sala, ila akilala vyengine vyovyote vile basi Udhu utatenguka Mtizamo wa Tano kama Ikiwa Atalala huju akiwa amesimama basi Udhu wake hautobatilika,lakini kama ikiwa vyenginevyo basi Udhu wake utatenguka.

Ambapo Mitizamo miwili kati ya hii imenukuliwa na Imam Al Rafii na myengine na Maimam wengineo. **Na mtizamo wa Kwanza Umenukuliwa na Imam Al Shashi Al Qaffal Al Marwazi katika Talkhis.**

Na Mtizamo sahih wa Madhhab ni Mtizamo wa kwanza, na Mitizamo myengine yote iliyobakia haina maana. Ambapo amesema Imam Al Shafii katika Al Umm na Al Mukhtasar, na Wanafunzi na Wafuasi wake kua: Inapendekezwa Kwa Mtu ambae anaweza kutia Udhu baada ya Kulala kwa aina yeyote ile kua atie Udhu kutokana na uwezekano wa kutokua Tohara, na hivyo kua ni mwenye kuepukana na tofauti za Wanazuoni.

Pia Imam Al Shafii amesema kua Udhu haubatiliki kwa kutokana na Kusinzia, na hii ndio Sunnah, na hakuna kutokukubaliana juu ya hili Na ushahidi wa hili ni Hadith ya Abd Allah Ubn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Sala*m alisimama katika Kusali Usiku hivyo nami nikasimama kushotoni mwake, lakini akanivuta nikae kulia kwake, na nilipokua nikisinzia alikua akinivuta ndewe ya sikio langu, na alikua akisali Rakaa 11*(Sahih Muslim)*

Imam Al Shafii na Wanafunzi wake wa Wafuasi wake wanasema kua: Tofauti baina ya Kulala na Kusinzia Ni kua Kulala hua kunauzidi nguvu za kiuwezo Ufahamu,na hivyo Mtu hua anapoteza uwezo wa Kuona, Kusikia n.k Wakati Kusinzia hua hakuuzidi nguvu Ufahamu bali hua kunazipunguza nguvu hisia lakini bila ya kuzipoteza.

Ambapo Imam Al Mutawwali na Qadhi Al Husayn wao wamesema kua Kulala hua ni Kuondokeaa na Hisia ndani ya Moyo na viungo vya Mwili kuregea. Na Imam Al Haramayn amesema kua: Kusinzia hukizidi Nguvu Kichwa na kusababisha sehemu ya Ubongo Inayohusiana na Hisia na chanzo cha mfumo wa neva kupoteza uwezo wa udhibiti na hivyo ukizidiwa basi na uwezo wa hiari hupungua.

Na huanzia kama Mvuke unaoteremka na kuuzidi Ufahamu na kusababisha hisia za Uregevu wa kivivu, na hii hua ndio kusinzia na hisia za Kusinzia. Na hisia za kusinzia zinapozidi nguvu ndio Usingizi hua unaanza kutawala, kisha kinachofuatia ni uregevu wa viungo vya mwili, na kiachfuata baada ya hapo ni Kuzama usingizini.

Na miongoni wa Dalili A Kusinzia ni kua na uwezo wa Kusikia kinachosemwa hata kama kisemwacho hua hakifahamiki.'*(Al Majmuu)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kutuambia kua: **'Kuota Ndoto hua ni Dalili ya Mtu kua Usingizini, na juu ya hili amesema Imam Al Shafii katika Kitabu chake cha Al Umm, na pia ametaja Imam Al Buwayti kama ilivyosemwa hapo kabla. Na hivyo Wanakubaliana kua Kama mtu akiwa na Uhakika kua Ameota lakini hana uhakika kama**

alilala kua Udhu wake Mtu huyo utakua umebatilika, lakini kama Mtu akiona kwenye Ufahamu wake na akawa hajui kua kama alichokiona ni kutokana na Ndoto au ni kutokana na mawazo yake, basi Udhu wa Mtu husika hautobatilika, kwa sababu kikanuni basi Udhu wake hua upo.

Na kama akiona kwenye Ufahamu wake huku akiwa hana uhakika kama alikua amelala au amesinzia, basi pia Udhu wake utakua haujabatilika, ambapo hata hivyo Imam Al Shafii amesema kua Kutia Udhu kutokana Na hali kama hizi hua ni bora kwa ajili ya kuchukua Tahadhari zaidi*(Al Umm)*

Hali ya tatu ni kua kama ikiwa Mtu ana uhakika kua alikua na usingizi lakini hana uhakika kua kuna uwezekano huo wa kulala ama la, basi udhu wake utakua bado upo. Na hivi ndivyo alivyosema Muandishi wa Al Bayan na Maimamu wengineo, na ndio Usahih.

Na hali ya Nne ni kua kama Mtu alipatwa na usingizi wakati akiwa amekaa kitako huku makalio au kalio limeachana na Ardhi basi kama ikiwa kuachana huko na Ardhi ilikua kabla ya kuamka basi Udhu utakua umebatilika, na hakuna uwezekano kua alikua hajalala.

Lakini kama ikiwa kuachana huko kumetokea baada ya kuamka, au katika wakati anaamka au hana uhakika kipi kitokea mwanzo baina ya mambo haya basi Udhu wake utakua haujabatilika.

Hali ya Tano ni kua kama Mtu amelala huku akiwa amekaa kitako na kuegemea Ukuta au kitu chengine kama hicho, basi Udhu wake hautobatilika Hata kama kitu alichokiegemea kitaanguka, na juu ya hili kuna Makubaliano juu yake miongoni mwa Wanazuoni wetu.
Na hali ya Sita ni kua Usingizi ni Usingizi kwetu sisi wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii, hivyo hakuna Usingizi mwepesi wala mzito kwani usingizi wa dakika moja na usingizi wa siku mbili hua ni Sawasawa kwa kila kitu.

Hali ya Saba ni kua Wanazuoni wetu wanasema kua hakuna tofauti kati ya Usingizi wa Mtu alielala huku akiwa amekaa kitako. Iwe kukaa huko ni kwa kukunja Miguu, amelalia Mgongo wake, au vyenginevyo lakini huku makalio yake yamagandamizana na sehemu aliyokalia juu ya Ardhi au juu ya Meli au kipando kama Ngamia au mnyama mwengine yeyote kua Udhu wake hautobatilika, na hivyo ndivyo alivyosema Al Shafii katika Kitab Al Umm na Wanazuoni wengine wa Madhhab ya Imam Al Shafii wamekubaliana nae.

Ama kama ikiwa Mtu atalala huku amekaa Kitako na kukumbatia Miguu yake, Amenyanyua Magoti yake n.k basi kuna Mitizamo Mitatu juu yake kama ilivyonukuliwa na Imam Al Mawardi na Imam Al Ruwayani. Ambapo Mtizamo wa kwanza ni kua Udhu haubatiliki kama kwa mtu aliekaa. Mtizamo wa pili ni kua unabatilika kama kwa mtu alielala. Mtizamo wa Tatu ni kua kama Makalio hayajashikamana na alichokikalia basi Udhu utabatilika, lakini kama yameshikamana basi hautobatilika ambapo mtizamo huu ni wa Imam Abu Fayyad Al Basri na ndio Anaoupendelea zaidi.

Hali ya Nane ni kua kama Mtu atalala chali na Makalio yameeshikamana na alichokilalia, basi inawezekana ikawa haitowezekana kubatilishika Udhu wake. Lakini hata hivyo Wanazuoni wetu wanakubaliana kua Udhu utakua umebatilika na hii ni kwa sababu hali hii hua si sawa na Mtu aliekalia Makalio yake.

Ambapo Imam Al Haramayn amesema haya katika Al Nihaya na katika Al Asalif kua juu ya hili kuna kutokukubaliana baina ya Wanazuoni wetu Kutokukubaliana ambako kunaweza kutafakkariwa, na hivyo kuthibitisha kua hakubatilishi Udhu.

Hali ya Tisa ni kua Msimamo Unaokubalika katika Madhhab yetu ni kama ilivyosemwa hapo kabla kua: Udhu wa mtu alielala huku akiwa amekaa Kitako basi Haubatiliki, iwe Mtu huyo yuko kwenye Sala ama la iwe Usingizi huo mwepesi au mzito. Ambapo imenukuliwa kwa Abu Musa Al Ashari *Radhi Allahu Anhu,* Imam Said Ibn Musayyib, Imam Majlaz na Hamid Al Araj kua: 'Usingizi haubatilishi Udhu hata kama Mtu awe amelala kabisa.'

Na Qadhi Abu Tayyib, Imam Is-haq Ibn Rahawayh, Imam Abu Ubyd Al Qasim na Imam Al Muzani wamesema kua: Udhu Hubatilika kwa Usngizi wa hali yeyote, na Imam Al Bayhaqi amenukuu haya kutokea kwa Imam Hasan Al Basr kwa Sanad inayoaminika.

Ambapo Imam Ibn Al Mundhir Al Nishapuri amesema kua: 'Hivyo pia ndivyo nisemavyo mimi, kwani Mtizamo huu pia umenukuliwa kutoka kwa Ibn Abbas, Anas, na Abu Hurayrah R*adhi Allahu Anhum.*'

Ambapo kwa upande wa Imam Malik na Imam Ahmad basi wao wanasema kua: 'Usingizi Mzito ndio unaobatilisha Udhu lakini si Mwepesi.'

Imam Ibn Al Mundhiri pia amenukuu juu ya hili kutoka kwa Imam Az Zuhri, Imam Rabiah na Imam Al Awzai.

Imam Abu Hanifa na Imam Daud wanasema kua: Kama Mtu akilala katika mikao ya Sala kama kusimama, kurukuu kusujudu n.k iwe anasali ama la basi udhu haubatiliki ila kama akilala utabatilka.' *(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kufafanua kwa kusema kua: '**Ama kuhusiana na Kupoteza Ufahamu kutokana na Sababu nyengine yeyote ile isiyokua Usingizi, yaani kama kuingia Wazimu, Kuzimia, Kulewa, Kuumwa n.k basi Udhu wa Mtu husika utakua ni wenye kubatilika.'**

Na hii ni kwa sababu kwa kua Udhu hubatilika kwa Usingizi, Basi bila ya Shaka itakua ni sababu tosha pia kubatilika kwake kutokana na hali za vitu kama hivyo. **Na hakuna tofauti juu ya hili baina ya Mtu aliekaa Kitako au aliesimama, kwani hali hizi hua ni tofauti na Usingizi.**

Kwa sababu Mtu alielala hua anaweza kuzungumza, na akiamshwa anaamka, na akitokwa na kitu wakati akiwa amekaa kitako basi atahisi, hivyo Mtu huyu hua tofauti na asiekua na akili au Alielewa Imam Al Shafii amesema kua Imesemwa kua ni Mara chache sana kwa Mtu anaerukwa na akili kua asitokwe na kitu katika sehemu za haja ndogo. Hivyo basi hua inapendekezwa pia Kukoga Janaba baada ya Kurudiwa na akili kama tahadhari*(Kitab Al Umm)*

Na Ummah unakubaliana kua Udhu hubatilika kwa kutokwa na akili au kuzimia, na Imam Ibn Al Mundhiri na Maimamu wengineo wamenukuu juu ya makubaliano haya.

Ambapo Wanazuoni wetu wa Madhhab ya Imam Al Shafii wao Wamenukuu kama uthibitisho Hadith ya Aisha *Radhi Allahu Anha* aliyosema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alizimia, kisha akapata Fahamu na akatia Udhu, kisha akazimia tena na akapata fahamu tena na akatia Udhu tena, (kama ilivyonukuliwa na Bukhari na Muslim)

Hivyo Wanazuoni wetu wanakubaliana kua yeyote yulw atakaepoteza Ufahamu kwa Kuzimia, Kulewa, Kuumbwa, Kurukwa na akili, Kunywa Dawa zitakazompotezea fahamu n.k basi Udhu

wake itabatilika Na hakuna kutokukubaliana juu ya hili isipokua juu ya Mtizamo wa Wanazuoni wa Khurasan usemao kua: Udhu wa Mtu alietumia Kilevi hua haubatiliki kama ikiwa ana ufahamu wake kiakili, kimatendo na kimaneno.

Ambapo Mtizamo huu umenukuliwa na Hujjat Ul Islami Imam Al Ghazali katika Al Basit, na Imam Al Furani, na Imam Al Mutawwali, Imam Al Ruwayni na wengineo. Jambo ambalo si sahih kwa sababu Kubatilika kwa Udhu hua kunategemeana na Kupoteza Ufahamu.' *(Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab)*

Na anasema Shaykh Ul Islami, Al Muhaqqiq Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: '**Jambo la Pili kinalobatilisha Udhu hua ni Kutokwa na Akili, yaani kupoteza uwezo wa kutofautisha baina ya mambo kutokana na Wazimu au Kuzimia, Kulewa n.k.**

Na anasema Al Abbab kua Akili hua ni Kitu bora zaidi ya Ilm kwa sababu Akili ndio Msingi na hivyo Ilm hutirirka kutokea Kwenye Akili kama vile Nuru inayotiririka kutoka kwenye Jua, na Muonekano kutokea kwenye Macho na hali kama hizo, akimaanisha asili ya Hitajio la Mtu, na *Allah Subhanah wa Ta'ala* hua anafahamika kutokana na akili na wala si kwa Ufahamu.'(*Tuhfah Al Muhtaj)*

Ambapo anasema Imam Abd Al Hamid Al Sharwani Al Shafii kua: '**Kilugha Akili hua inamaanisha Kinga, kwa sababu Akili hua inamkinga Mtu kutokana na Kufanya Maasi**, **ama kitaalamu basi ufafanuzi bora wa Akili ni kama alivyosema Imam Al Shafii kua hua ni Sifa ambayo inampelekea mtu kuweza kutofautisha baina ya Jema na Ovu.'***(Hashiyah Al Sharwani)*

Anasema pia Muwaffaqah Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Kupoteza Fahamu Kutokana na Kuzimia, Kulewa na kutumia Dawa ambazo zinasababisha kupotea kwa fahamu hua kunabatilisha Udhu kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni, kwani Imam Ibn Al Mundhiri anasema kua Wanazuoni wanakubaliana kua Atakaezimia basi anatakiwa atie Udhu Kwani Watu wanaopoteza Ufahamu kwa kutokana na hali hizi hua ni wenye Kupoteza Ufahamu zaidi kuliko Mtu alielala, na hii ni kutokana na ukweli ni kua hata kama wakizinduliwa basi hawazinduki, na kutokana na kua Udhu unahitajika kwa alielala, basi hua unamuwajibikia kila aliingia kwenye hali nzito zaidi ya kupoteza fahama kuliko Usingizi.'**(*Al Mughni)*

Naam..Hivyo basi Wanazuoni wanakubaliana kua Kupoteza Ufahamu iwe kwa Kulala, Kulewa, Kuzimia, Kunywa Sumu, Kunywa Dawa, Kupigwa Sindano kwa ajili ya Matibabu, Kupandisha Shaytani, Kurukwa na akili n.k hata iwe kwa sekunde 5, basi hua kunabatilisha Udhu.

MUBTILAT SALAT – IRTIDDAD - KUTOKA KWENYE UISLAM

❖❖❖❖

Neno *Radda* kwa Lugha ya Kiarabu hua ni lenye kumaanisha Kurudisha, Kugeuza, Kukataa, Kusukuma, Kuchukua tena, Kutoa tena.

Neno Radda ndi lililotoa neno *Taradda* lenye kumaanisha kusita sita, kuenda huku na kurudi kule, na pia neno Radda likatoa neno *Irtiddad* ambalo humaanisha Kurudi katika hali ya mwanzoni kabisa.

Qur'an imetumia asili ya neno Radda mara kadhaa ikiwemo pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kuhusiana na Nabii Musa kua:

﴿فَرَدَدْنَاهُ إِلَىٰ أُمِّهِ كَىْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلاَ تَحْزَنَ وَلِتَعْلَمَ أَنَّ وَعْدَ ٱللَّهِ حَقٌّ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لاَ يَعْلَمُونَ﴾

Faradadnahu ila ommihi kay taqarra AAaynuha wala tahzana walitaAAlama anna waAAda Allahi haqqun walakinna aktharahum la yaAAlamoona *(SuratAl Qasas 28:13)*

Tafsir: ***Hivyo tukarudisha kwa Mama yake, ili apate kufurahi na asiweze kua na huzuni na apate kujua kua Ahadi ya Allaj ni ya kweli, lakini wengi si wenye kujua.***

Na pia pale ziliposema kuhusiana na Nabii Sulayman na Farasi wake kua:

﴿رُدُّوهَا عَلَيَّ فَطَفِقَ مَسْحاً بِٱلسُّوقِ وَٱلأَعْنَاقِ﴾

Ruddooha AAalayya fatafiqa mashan bialssooqi waal-aAAnaqi).*(Surat Sad 38:33)*

Tafsir: ***Kisha akasema (Nabii Sulayman): 'Warudishe (Farasi) kwangu Mimi' na kisha akaanza kuwapapasa Miguuni mwao na Shingoni mwao.***

Na pale ziliposema aya kua:

﴿ثُمَّ رُدُّوۤاْ إِلَىٰ ٱللَّهِ مَوْلاَهُمُ ٱلْحَقِّ أَلاَ لَهُ ٱلْحُكْمُ وَهُوَ أَسْرَعُ ٱلْحَاسِبِينَ﴾

Thumma ruddoo ila Allahi mawlahumu alhaqqi ala lahu alhukmu wahuwa asraAAu alhasibeena*(Surat Al An Aaam 6:62)*

Tafsir: ***Na kisha watarudishwa kwa Allah, Mola wao Hakimu muadilifu, Kwa hakika Hukumu ni yake n ani mwepesi wa kuhesabu.***

Ambapo anasema Imam Raghib Al Isfahani kua: **'Neno *Radda* hua linamaanisha Kuepuka au Kurudisha Kitu Kutoka katika Hali moja kuingia Katika Hali nyengine**. **Hivyo Mtu anaweza kusema Radadtuhu kumaanisha Nimekigeuza au Nimekirudisha**. **Na inaposemwa Irtadda basi humaanisha Imerudishwa.'**

Qur'an imetumia pia asili ya neno Radda mara kadhaa ikiwemo pale aliposema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ آمَنُواْ ثُمَّ كَفَرُواْ ثُمَّ آمَنُواْ ثُمَّ كَفَرُواْ ثُمَّ ٱزْدَادُواْ كُفْراً لَّمْ يَكُنِ ٱللَّهُ لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلاَ لِيَهْدِيَهُمْ سَبِيلاً﴾

Inna alladheena amanoo thumma kafaroo thumma amanoo thumma kafaroo thumma izdadoo kufran lam yakuni Allahu liyaghfira lahum wala liyahdiyahum sabeelan*(Surat An Nisaa 4:137)*

Tafsir - ***Kwa Hakika Wale Walioamini Kisha Wakakufuru Kisha Wakaamini tena Kisha Wakakufuru Kisha Wakazidi Kukufuru Basi Allah Hatokua na Msamaha kwao. Na Wala Hatawongoza Njia.***

Na pia katika aya isemayo:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَصَدُّواْ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ وَشَآقُّواْ ٱلرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ ٱلْهُدَىٰ لَن يَضُرُّواْ ٱللَّهَ شَيْئاً وَسَيُحْبِطُ أَعْمَالَهُمْ﴾

Inna alladheena kafaroo wasaddoo AAan sabeeli Allahi washaqqoo alrrasoola min baAAdi ma tabayyana lahumu alhuda lan yaduroo Allaha shay-an wasayuhbitu aAAmalahum. (*Surat Muhammad 47:32)*

*Tafsir: **Kwa Hakika wale waliokufuru Na Wakawazuia Watu kutokana na Njia ya Allah Na Wakamtilia Shaka Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam Baada ya Kubainishwa kwao wao Njia Hawatomdhuru Allah kwa Chochote bali Atazifuta Amali zao***

Na akasema tena A*llah Subhanahu wa Ta'ala* kua:

﴿وَمَن يَرْتَدِدْ مِنكُمْ عَن دِينِهِۦ فَيَمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُوْلَٰٓئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَٰلُهُمْ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْأَخِرَةِ ۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ﴾

Waman yartadid minkum AAan deenihi fayamut wahuwa kafirun faola-ika habitat aAAmaluhum fee alddunya waal-akhirati waola-ika as-habu alnnari hum feeha khalidoona. *(Surat Al Baqara 2:217)*

Tafsir: **Na Atakaetoka Miongoni mwenu katika Dini yake Na Kisha akafariki huku akiwa Kafiri basi Atakua amepoteza Amali zake Hapa Duniani na Akhera Na Watakua ni watu wa Motoni Ambapo Watakaa ndani yake Milele.**

Na akasema tena kua:

﴿وَلَقَدْ أُوحِىَ إِلَيْكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكَ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ﴾

Walaqad oohiya ilayka wa-ila alladheena min qablika la-in ashrakta layahbatanna AAamaluka walatakoonanna mina alkhasireena*(Surat Az Zumar 39:65)*

Tafsir: **Na Kwa Hakika Sisi tumekushushia juu yako (Ewe *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam* Na Wale waliotangulia Kabla Yako kua Kama Ukinishirikisha Basi Nitazibatilisha Amali zako Na Utakua Miongoni mwa waliokula Hasara.**

Hivyo hizi ni aya zinazozungumzia kuhusiana na wenye kufanya Irtiddad yaani Kuhama kutoka katika Imani ya Dini ya Uislam na kuingia au kurudi kwenye Ukafiri. Ambapo Wanazuoni wanapozungumzia Hali hizi hua wanatumia maneno Al Riddah au Al Irtidad ambayo humaanisha Kuachana na Kitu baada ya Kukifikia.

Kwani neno Al Irtiddad hua ni sawa kimaana na neno Al Riddah, mbali ya kua Al Riddah hua linatumika zaidi kwa ajili ya kunashibishwa na Imani ya Kiislam na neno Al Itriddad hua linatumika kunasibishwa na mambo mengineyo pia, lakini kwa upande wa Qur'an basi maneno mawili haya hua yanatumika katika matumizi yenye kuhusiana na hukmu za sharia za Imani ya Dini ya Kiislam, kwa mfano kwa mtu mwenye kutoka katika Uislam, kua ni mwenye kubatilisha jitihada zake zote katika ufanyaji wa Amali zake alizozifanya wakati akiwa Muislam kabla ya kujitoa katika Uislam.

Hivyo, baada ya kuangalia baadhi ya Aya zenye kuzungumzia kuhusiana na Kubatilika kwa Amali zote za wale watakaofanya Irtidad yaani watakaotoka katika Imani ya Dini ya Kiislam, na kuingia kwenye Imani ya Kikafiri kwa kufanya Irtidad kwa kupitia kwa moja kati ya mambo manne yafatayo:

1-Kufanya Irtidad ki Imani yaani kwa Kumshirikisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Miungu wengine, Kukana kuwepo kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Kukana Sifa zake na Majina yake Matukufu, Kumsingizia Sifa zisizokua zake, kama Kua na Mtoto,Kutoamini Siku ya Malipp, Kutoamini Kuwepo kwa Mitume yake, Kutoamini kuwepo kwa Ulimwengu wa Al Ghayb, Kutoamini Vitabu vyake n.k.

2-Kufanya Irtidad kwa Kauli kwa Mfano Kumkashifu kwa Maneno *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Mitume wake, au Mtume wake *Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam.*

3-Kufanya Irtidad kwa Vitendo kwa mfano Kuchoma Moto Qur'an ambayo haijaharibika, Kuitia Najis Qur'an, Kusujudia Masanam, n.k.

4-Kufanya Irtidad kwa Kufuta Nguzo za Dini Ya Kiislam na Kuachana nayo kwa Kutoihesabu kua ni Nguzo ya Dini ya Kiislam.

Hivyo Muislam yeyote atakaefanya Moja kati ya Mambo hayo yenye sifa za kua ni kufanya Irtidad juku akiwa amefanya hivyo kwa hiari yake na wa akili zake basi hua ni mwenye Kujitoa katika Imani ya Dini ya Kiislam. Na Wanazuoni wanakubaliana kua Mtu anaetoka Katika Uislam basi hua ni mwenye Kujibatilishia pia haki juu ya mambo yafuatayo:

1-Kufutika na Kubatilika kwa Ibada zote za mhusika alizofanya wakati akiwa Muislam.

2-Kubatilika kwa Ndoa Mtu Husika hapo hapo mara tu baada ya kutoka kwenye Uislam.

3-Kufutika kwa Udugu wa Mhusika na Familia yake yote kunakopelekea kubatilika kwa Mirathi ya Mtu husika kutoka katika Mali za Waislam.

4-Kutostahiki Kusaliwa kwa Maiti yake na Waislam, na pia kutoruhusika Kuzikaa kwa Maiti yake kwenye Makaburi ya Kislam.

Hivyo Hukmu za Sharia ya Kiislam kuhusiana na kufutika kwa Amali na Haki za Kiislam juu yake zitakua ni zenye Kutekelezeka bila kihitajika Msimamizi wa Utekelezwaji wa Hukmu za Kiislam kwa mfano labda Qadhi au Kiongozi Muadilifu wa Kiislam.

Na kama tulivyoona kwenye Aya hapo kabla kama Aya ya 217 ya Surat Al Baqara, Aya ya 137 ya Surat An Nisaa, Aya ya 65 ya Surat Az Zumar, Aya ya 32 ya Surat Muhammad kua Kama Mtu huyo hakutubu na hakurudi katika Uislam basi Allah Subhanah wa Ta'ala Hatamuongoza Njia Sahih na wala hatomsamehe na kisha katika Siku ya Malipo atamuingiza katika Moto wa Jahannam ambayo ni mafikio yenye Adhabu kali sana ndani yake.

Na mbali ya kua Wanazuoni wanakubaliana juu ya Hukmu za kubatilika kwa Amali na Haki za Mtu mwenye Kutoka kwenye Uislam. Lakini hata hivyo Wanazuonumi wametofautiana kuhusiana na Suali la kua Jee kufanya Irtiddad kunabatilisha Udhu ama la. Kwani imesemwa katika *Mawsuah Ahkami Fiqhiyyah kua:*

Ama kuhusiana na Kutoka kwenye Uislam kua ni kwenye Kupelekea kubatilika kwa Udhu wa Mtu husika ama la basi kuna Mitizamo miwili ifuatayo juu yake.

1-Irtiddad hua inabatilisha Udhu ambapo huu ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na pia kuna Mtizamo mmoja wa Mwanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, na pia ndio Mtizamo wa Wanazuoni wa Vizazi vya Mwanzoni mwa Uislam Ambapo wao Wamesimamia katika Uthibitisho wa Aya ya 5 ya Surat Al Maidah isemayo:

﴿وَمَن يَكْفُرْ بِٱلْإِيمَٰنِ فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهُۥ وَهُوَ فِى ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ﴾

Waman yakfur bial-eem<u>a</u>ni faqad <u>h</u>abi<u>t</u>a AAamaluhu wahuwa fee al-<u>a</u>khirati mina alkh<u>a</u>sireena(*Surat Al Maidah 5:5)*

Tafsir: ***Na Atakaekufuru Imani Basi Amali zao zote zitakua Bure na Akhera Atakua miongoni mwa waliokula hasara.***

Na pia Ushahidi wa Aya nyenginezo tulizoziangalia hapo kabla.Ambapo Aya hizi zinathibitisha kua Udhu ni miongoni mwa Amali Njema na hivyo Kutoka katika Uislam hua kunabatilisha Amali zote njema.

Na pia kutokana na Uthubitisho wa Hadith isemayo kua:

عن أبي مالك الحارث بن عاصم الأشعري رضي الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم : "الطهور شطر الإيمان، والحمد لله تملأ الميزان، وسبحان الله والحمد لله تملآن -أو تملأ- ما بين السماوات والأرض، والصلاة نور، والصدقة برهان، والصبر ضياء، والقرآن حجة لك أو عليك. كل الناس يغدو، فبائع نفسه فمعتقها، أو موبقها" ((رواه مسلم)).

Amesema Abu Malik Al Al Harith Ibn Assam Al Ashari *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Tohara ni Nusu ya Imani, na Alhamd lillah inajaza uzito wa Mezani, na Subhanah Allah inajaza kile kilichomo baina ya Mbingu na Ardhi Na Sala ni Nuru, Sadaka ni Uthibitisho, Subira ni Taa na Qur'an ni Hoja kwa ajili yako au dhidi yako, Na Watu hutoka nje Asubuhi na kuziuza Nafsi zao, aidha kwa Kuziachia Huru au kwa Kuziangamiza.*(*Sahih Muslim)*

Ambapo kutokana na Hadith hii basi ni kua kama Udhu hua ni Nusu ya Imani, na Irtiddad hua Kunabatilisha Imani, basi inamaanisha kua Udhu unabatilka kutokana na mtu kutoka kwenye Uislam,kwani ni Udhu ni Nusu ya Imani.

2-Mtizamo wa pili ni kua Irtiddad hua haibatilishi Uduu, ambapo huu ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii, baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik na pia ndio Mtizamo wa Imam Ibn Hazim.

Ambapo Mtizamo wa Wanazuoni hawa unasimamia kwenye aya ya *Surat Al Baqara* isemayo kua:

﴿وَمَن يَرْتَدِدْ مِنكُمْ عَن دِينِهِۦ فَيَمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَأُوْلَٰٓئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَٰلُهُمْ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ ۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ﴾

Waman yartadid minkum AAan deenihi fayamut wahuwa kafirun faola-ika habitat aAAmaluhum fee alddunya waal-akhirati waola-ika as-habu alnnari hum feeha khalidoona*(Surat Al Baqara 2:217)*

Tafsir: **Na Atakaetoka Miongoni mwenu katika Dini yake Na Kisha akafariki huku akiwa Kafiri basi Atakua amepoteza Amali zake Hapa Duniani na Akhera Na Watakua ni watu wa Motoni Ambapo Watakaa ndani yake Milele.**

Ambapo aya hii inathibitisha kua Irtiddad hua inabatilisha Amali njema zote lakini pale itakapokua Mtu husika hakutubu na kisha akafariki huku akiwa katika hali hio ya Kutokua Muislam.

Na hakuna Aya wala Hadith Dhaifu wala sahih wala Makubaliano ya Wanazuoni yanayothibitisha kua Kutoka kwenye Uislam kunabatilisha Udhu, na Wanazuoni wanakubaliana kua Kutoka katika Uislam hakubatilishi Tohara ya Janaba, wala ya Hedhi, wala Nifasi wala Kuachiwa Huru kwa Mtumwa hapo kabla, hivyo Jee itakuaje kubatilishe Udhu?'*(Mawsuah Ahkami Fiqhiyyah)*

Kwani tunapozungumzia Kuhusiana na Al Irtiddad yaani Kutoka Katika Imani ya Dini ya Kiislam basi Wanazuoni wanakubaliana kua hali hio hua imegawika katika Hali Tatu zifuatazo:

1-Kivitendo.

2-Kimaneno.

3-Kiimani.

Ambapo hali tatu hizi hua zinajitegemea kila moja kivyake. Yaani, Al Irtiddad ya hali ya Maneno hua ni Kujitoa kwenye Imani ya Dini ya Kiislam kwa njia ya kusema maneno ya Irtiddad bila ya Kufanya Kitendo wala Kuamini kile unachokisema.

Al Irtiddad ya kujitoa kwenye Uislam kwa Kitendo hua ni Kujitoa kwenye Dini ya Kiislam kwa Kufanya kitendo cha Al Irtiddad hata kama hukusema Kitu katika Kufanya Kitu hicho au huamini Kitu hicho.

Na Irtiddad ya Kujitoa kwenye Dini ya Kiislam kwa Kuamini kisichotakiwa kuamini hua ni Irtiddad hata kama hukufanya kwa kitendo au hukusema juu yake.

Ambapo Juu ya hali hizi za Irtiddad basi Wanazuoni Wanakubaliana kua huhesabiwa kua ni hali ya Irtiddad hata kama Mtu hajui Hukumu ya Kufanya Irtiddad, au hata kama Mtu husika alikua anatania au alikua na Hasira.

Kwani imesemwa kwenye Mawsuat *Fiqhiyyah Al Kuwatiyyah* kua: '**Wengi Miongoni mwa Wanazuoni wanakubaliana kua Mtu mwenye Hasira hua anahesabiwa juu ya ayasemayo na ayafanyayo katika wakati akiwa kwenye hasira. Hivyo anahesabiwa juu ya matendo yake ayafanyayo kama Kukufuru, Kuua, Kudhulumu, Kutoa Talaka, Kuachia Huru Mtumwa, Kuweka Nadhiri n.k.'***(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyah)*

Na amesema Imam Al Muhakkikiin Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: **'Kama Mtu akisema kua Mimi si Miongoni mwa Ummah wa Muhammad Au labda Mimi siyajui Kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* au Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam,* au Mimi si Muislam, au Mimi siko pamoja na Uislam, basi mtu huyo hua amefanya Irtiddad, amejitoa katika Uislam na ni Kafiri'***(Al Aalam Bi Qawwati Al Islam)***

Na amesema Imam Ibn Abd Al Barr kua: **'Amesema Imam Is-haq Ibn Rahawayh kua: Wanazuoni wanakubaliana kua Mtu yeyote yule atakaemkashifu *Allah Subhanah wa Ta'ala* au Mtume wake *Salallahu Alayhi wa Salam,* au atakaekataa juu ya kitu ambacho *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekielezea, au atakaemuua Mtume wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* huku akiwa anaamini juu ya alichokiteremsha *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Mtu huyo atakua ni Kafiri***(At Tahmid)***

Kwani anasema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ۚ قُلْ أَبِٱللَّهِ وَءَايَٰتِهِۦ وَرَسُولِهِۦ كُنتُمْ تَسْتَهْزِءُونَ ۝ لَا تَعْتَذِرُوا۟ قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَٰنِكُمْ ۚ إِن نَّعْفُ عَن طَآئِفَةٍ مِّنكُمْ نُعَذِّبْ طَآئِفَةً بِأَنَّهُمْ كَانُوا۟ مُجْرِمِينَ﴾

Wala-in saaltahum layaqoolunna innama kunna nakhoodu wanalAAabu qul abiAllahi waayatihi warasoolihi kuntum tastahzi-oona. La taAAtadhiroo qad kafartum baAAda eemanikum in naAAfu AAan ta-ifatin minkum nuAAaththib ta-ifatan bi-annahum kanoo mujrimeena*(Surat At Tawbah 9:65-66)*

*Tafsir: **Na Ukiwauliza Watasema: Tunazungumza na Kutania Tu Waambie (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Kwa ajili ya Allah na Dalili zake? Na Mtume wake Ambavyo Nyinyi Mnafanya Mzaha juu yake? Msitafute Udhuru Kwani Mmekufuru baada ya Kuamini Tukikusameheni baadhi yenu . Basi Tutawaadhibu Baadhi Miongoni mwenu Kwa Sababu ya kua ni Wenye Kukufuru***

Ambapo amesema Mwanafunzi wa Imam Al Ghazali Al Shafii ambae ni Al Qadhi Imam Abu Bakr Ibn Arabi Al Maliki kuhusiana na Aya hizi za Surat At Tawbah kua; '**Wanachokisema Chochote kile kiwe ni cha Matani au ni kweli basi hua ni Kujitoa katika Uislam, na hakuna kutokukubaliana miongoni mwa Wanazuoni wa Ummah huu juu ya hilo. Kwani Ukweli hua Ndugu yake ni Haki na Ilm, na Uongo hua Ndugu yake ni Batili na Ujinga.**'*(Ahkami Al Qur'an)*

Na kuna hadith isemayo kua

حَدَّثَنِي عَبْدُ اللَّهِ بْنُ مُنِيرٍ، سَمِعَ أَبَا النَّضْرِ، حَدَّثَنَا عَبْدُ الرَّحْمَنِ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ ـ يَعْنِي ابْنَ دِينَارٍ ـ عَنْ أَبِيهِ، عَنْ أَبِي صَالِحٍ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَ " إِنَّ الْعَبْدَ لَيَتَكَلَّمُ بِالْكَلِمَةِ مِنْ رِضْوَانِ اللَّهِ لاَ يُلْقِي لَهَا بَالاً، يَرْفَعُ اللَّهُ بِهَا دَرَجَاتٍ، وَإِنَّ الْعَبْدَ لَيَتَكَلَّمُ بِالْكَلِمَةِ مِنْ سَخَطِ اللَّهِ لاَ يُلْقِي لَهَا بَالاً يَهْوِي بِهَا فِي جَهَنَّمَ

Amesema Abd Allahi Ibn Munir kua nimemsikia Aba Nasir kua amesema Abd Rahman Ibn Abd Allah yaani Ibn Dinar kua amesema Baba yake kua amesema Abi Salih kua amesema Abu Hurayrah kua Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Mja wa Allah anaweza akasema Neno ambalo litamfurahisha Allah, bila ya Mtu huyo kulitilia maanani neno hilo, na kutokana na neno hilo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamnyanyua Darja yake Mtu huyo.

Na Mja wa Allah anaweza akasema neno bila kulitilia manani, lakini neno hilo likamkasirisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* na hivyo kutokana nalo neno hilo basi *Allah Subhanah wa Ta'ala* atamtia Motoni Mtu huyo.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Na akasema Imam Muhammad Ibn Jarrir At Tabari Al Shafii kua: **'Kuna baadhi ya Waislam ambao hua Wanajitoa Katika Dini ya Kiislam bila ya Kukusudia Kujitoa'***(Tahdhib Al Athar)*

Allah ateupushe nao watu hao..Allahuma Amiin.

Na akasema Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii kua: **'Imam Al Haramayn amenukuu kutoka kwa Wanazuoni wa Usul Ul Fiqh kua Yeyote yule atakae tamka neno la Irtiddad hata kama akijidai kua ametumia maana ya Utata wa ndani yake neno hilo basi hua Amejitoa katika Uislam kimwili na kiroho.'***(Al Zawajir)*

Imam Ibn Nujaym kua: **'Yeyote yule atakaesema Neno la Kukufuru iwe kwa kutania au kwa mchezo basi hua amefanya Irtiddad na Imani yake hua imepotea.'***(Bahr Al Raiq Kanz Ad Daqaiq)*

Na akasema Imam Abu Bakr Al Jassas Al Hanafi kua: **'Kutania, Kucheza na Kweli hua ni sawia pale inapokua ni kuhusiana na Irtiddad bila ya Kulazimishwa kwa Sababu Wanafiq waliotajwa kwenye Aya wamesema walichokisema kwa Matani, hivyo Allah akawashushia Aya kuonesha kua Imani yao ni ya Utani.'***(Ahkam Al Quran Al Fusuu Fi Usul)*

Amesema Imam Abd Allah Ibn Husein Ibn Tahir Al Alawi Al Hadhrami Al Shafii kua: **'Ni wajibu kwa kila Muislam kuilinda na kuihifadhi Imani yake ya Dini ya Kiislam kutokana na kile Kitakachoiharibu, Kitakachoibatilisha na Kuikata ambacho ni Al Irtiddad.'**

Kiasi ya kua baadhi ya Watu wanazungumza maneno ambayo huwatoa nje ya Imani ya Dini ya Kiislam, na wao hawaoni kua jambo hili ni Dhambi wachilia mbali kua ni Kukufuru.

Ambapo hii hua ni Uthibitisho wa Kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliposema kua: Mja atasema Jambo ambalo ataona kua halina madhara, lakini matokeo yake litamzamisha kwenye kina cha Ghorofa 70 za Moto

Allah atunusuru, Kwani katika zama zetu imekua kuna udharau wa Kauli Yaani Al Irtiddad, umbali wa masafa miaka 70 ya kushuka chini, na hii ni sehemu ya kina cha chini kabisa ya Moto, ambayo ni maalum kwa Makafiri.

Hadith hii imenukuliwa na Imam At Tirmidhii na amesema kua ni Hasan Hadith, na pia kuna hadith kama hii iliyonukukiwa na Imam Bukhari na Imam Muslim.

Hadith hii inathibitisha kua ni rahisi sana kwa Mtu kutumbukia kwenye Kufuru, kwani hua hakuna ulazima wa kua ni mwenye kujua Hukmu, au kua na Moyo safi au kujua maana Ya maneno na kuyaamini.'*(Sulam Al Najat Illa Mahabati Allahi Haqqan)*

Na amesema Imam Al Bakri Al Dimyati Al Shafii kua: **'Fahamu kua watu wengi wa kawaida hua wanasema maneno kadhaa ambayo ni yenye kujumuisha aina za Kufuru, bila ya wao kujua kua yanamaanisha hivyo hua ni Wajibu kwa Watu Wenye Ilm kuwaelemisha watu hawa ili wapate kuepukana nayo maneno hayo.**

Kwani kama ikiwa wanayajua maneno hayo na kuyasema basi hua wanajibatilishia Amali zao Na si hivyo tu bali pia wanajiingiza kwenye Adhabu kali sana inayoumiza sana. **Hivyo Kujua haya hua ni Muhimu sana kwa sababu asielijua Ovu basi huangukia ndani yake kirahisi bila kujijua**. **Na Maovu yote hua yanasababishwa na Ujinga, na Mema yote hua yanasabisishwa na Ilm, kwani Ilm ni Nuru iliyodhahiri na Ujinga ni Mwenza mbaya sana.'***(Ianat At Talibin aAla Al Fadh Fat-h Muin)*

Na imesemwa katika Fatawa Al Hindiyah kua: '**Yeyote yule atakaetamka Maneno ya Kufuru bila ya kujua kua ni Kufuru lakini akatamka kwa Hiari yake, basi hua ni mwenye kuhesabiwa kua ni mwenye Kufanya Irtaddad, na hii ni kulingana na Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni, hivyo mtu huyo hua hasameheki kutokana na kisingizio cha kua hakujua.'***(Fatawa Al Hindiyyah)*
Na amesema Imam Al Muhakkikiin Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii kua: '**Yeyote yule atakaetamka maneno ya Kufuru au atakaefanya kitendo cha Kufuru au atakaeamini juu ya Kufuru huku akiwa ni Mjinga asiejua juu ya Kufuru hio basi hua hana kisingizio na huhesabiwa kua amefanya Irtiddad na ni Kafir**i.'*(Fatawa Al Kubra Al Fiqhiyyah)* Na huo ndio pia Mtizamo wa Imam Al Qadhi Iyad Al Maliki.

Naam..tunakumbushana haya kwa sababu anasema Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Imam Ahu Fadhl Abd Rahman Ibn Abi Bakr Ibn Muhammad Jalal Al Din Al Suyuti Al Shafii kua: '**Yeyote yule ambae hajui juu ya Uharamu wa kitu kinachofanywa na wengi kati ya Watu katika Jamii yake, basi hakitokubaliwa kisingizio chake, isipokua labda kama Mtu huyo atakua ndio kwanza ameingia kwenye Uislam au anakaa mbali sana na Watu labda Jangwani ambako hakuna mambo yaliyoharamishwa kwa mfano kama Zinaa, Mauaji, Wizi, Ulevi, Kuzungumza ndani ya Sala, Kula mchana katika mwezi wa Ramadhani, n.**k.'*(Ashbah Wa Nazair)*

Naam, tuko katika kufahamishana kuhusiana na Al Irtiddad, au Al Ridda yaani Kujitoa katika Imani ya Dini ya Kiislam ambako hua ni aidha kwa njia ya Maneno, Vitendo au Imani. Na kuhusiana na Kufuru ya Kauli basi na tufafanue Mfano wa Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا قُتَيْبَةُ، حَدَّثَنَا أَبُو خَالِدٍ الأَحْمَرُ، عَنِ الْحَسَنِ بْنِ عُبَيْدِ اللَّهِ، عَنْ سَعْدِ بْنِ عُبَيْدَةَ، أَنَّ ابْنَ عُمَرَ، سَمِعَ رَجُلاً، يَقُولُ لاَ وَالْكَعْبَةِ . فَقَالَ ابْنُ عُمَرَ لاَ يُحْلَفُ بِغَيْرِ اللَّهِ فَإِنِّي سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه

وسلم يَقُولُ " مَنْ حَلَفَ بِغَيْرِ اللَّهِ فَقَدْ كَفَرَ أَوْ أَشْرَكَ " . قَالَ أَبُو عِيسَى هَذَا حَدِيثٌ حَسَنٌ . وَفُسِّرَ هَذَا الْحَدِيثُ عِنْدَ بَعْضِ أَهْلِ الْعِلْمِ أَنَّ قَوْلَهُ " فَقَدْ كَفَرَ أَوْ أَشْرَكَ " عَلَى التَّغْلِيظِ . وَالْحُجَّةُ فِي ذَلِكَ حَدِيثُ ابْنِ عُمَرَ أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم سَمِعَ عُمَرَ يَقُولُ وَأَبِي وَأَبِي . فَقَالَ " أَلاَ إِنَّ اللَّهَ يَنْهَاكُمْ أَنْ تَحْلِفُوا بِآبَائِكُمْ " . وَحَدِيثُ أَبِي هُرَيْرَةَ عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم أَنَّهُ قَالَ " مَنْ قَالَ فِي حَلِفِهِ وَاللاَّتِ وَالْعُزَّى فَلْيَقُلْ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ " . قَالَ أَبُو عِيسَى هَذَا مِثْلُ مَا رُوِيَ عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم أَنَّهُ قَالَ " إِنَّ الرِّيَاءَ شِرْكٌ " . وَقَدْ فَسَّرَ بَعْضُ أَهْلِ الْعِلْمِ هَذِهِ الآيَةَ : (وَمَنْ كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلاً صَالِحًا) الآيَةَ قَالَ لاَ يُرَائِي

Amesema Qutaybah kua, Abu Khalid al-Ahmar amesema kua, kutoka kwa al-Hasan Ibn Ubaydullah, kutoka kwa Sa'd ibn Ubaydah, kwamba Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* alimsikia mtu akisema, "Naapa, kwa Al Ka'bah." Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema: "Mtu asiape kwa asiyekuwa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwani nilimsikia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akisema, 'Mwenye kuapa kwa asiyekuwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekufuru au amefanya shirki.'"

Imam Abu Isa Al Tirmidhii akasema, "Hii ni hadithi nzuri. Hadithi hii imefasiriwa na baadhi ya Wanazuoni kuwa kauli yake, "Basi amefanya Ukafiri au Ushirikina," ni adhabu kali. Ushahidi wa hili ni Hadith ya Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu,* kwamba *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimsikia Umar *Radhi Allahu Anhu* akisema, "Naapa kwa Baba yangu."

Basi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kuapa kwa Baba zenu. Na Hadithi ya Abu Hurayrah kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo: "Mwenye kutaka kusema kua Ameapa kwa Al-Lat na Al-Uzza, basi na aseme: "Hapana Mungu Ila Allah'.

Imam Abu Isa At Tirmidhi amesema, "Hii ni sawa na ilivyopokewa kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwamba alisema, 'Kujionyesha ni ushirikina.'" Baadhi ya wanachuoni wameifasiri Aya hii: "Na mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi na afanye vitendo vyema," Aya hiyo akasema, "Asijionee.'*(Jamii At Trimidhii, Sunnan Abu Daud, Musnad Imam Ahmad)***

Ambapo hii ni Hadith inayosisitiza Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kuhifadhi Sifa ya Umoja wa *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Ambapo amesema Imam Ibn Abd Al Barr kua: **'Hadith hii inabeba Ujumbe unaobainisha kua Hairuhusiki Kuapa kwa hengine chochote zaidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* kuhusiana na Kitu chochote au jambo lolote au hali yeyote, na Juu ya hili kuna makubaliano ya Wanzuoni Juu yake.'***(Al Tahmid)*

Ambapo amesema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Maneno yasemayo kua Amemshirikisha Allah katika Hadith hii yanamaanisha Onyo linabainisha Ukubwa wa Uovu wa Kuapa kwa Maneno husika**. **Ambapo wale wanaosema kua Imeharamishwa ndio wameshikamana na Uthibitisho huo. Ambapo kuhusiana na Kuapa na vyenginevyo yaani zaidi ya**

Majina na Sifa za *Allah Subhanah wa Ta'ala*, basi imethibitishwa kua ni Haram Imekatazwa.' *(Fat-h Al Barr)*

Na anasema Imam Al Haramayn Al Shafii kua: 'Kama mtu atakua anakiamini kile anachokiapia na kukitukiza kama anavyomuamini *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi Kuapa kwake huko itakua ni Haram na Mtu huyo atahesabiwa kua ametoka katika Uislam kutokana na imani hio.'*(Fat-h Al Barr)*

Na anasema Imam Al Bukhari kua:

حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ مَسْلَمَةَ، عَنْ مَالِكٍ، عَنْ نَافِعٍ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ ـ رضى الله عنهما ـ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم أَدْرَكَ عُمَرَ بْنَ الْخَطَّابِ وَهْوَ يَسِيرُ فِي رَكْبٍ يَحْلِفُ بِأَبِيهِ فَقَالَ " أَلاَ إِنَّ اللَّهَ يَنْهَاكُمْ أَنْ تَحْلِفُوا بِآبَائِكُمْ، مَنْ كَانَ حَالِفًا فَلْيَحْلِفْ بِاللَّهِ، أَوْ لِيَصْمُتْ ".

Amesema Abd Allah Ibn Masalamh kua Amesema Malik kua amesema Nafii, kua amesema Amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikutana na Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* wakati alipokua anaenda kwa Kundi la watu waliopanda Ngamia huku akiapa kwa Kupitia kwa Baba yake: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Loh! Allah amekukatazeni Kuapa kwa Kupitia kwa Baba zao, Hivyo atakaeapa basi na aape kwa Jina la Allah Au akae Kimya asiape.'*(Sahih Bukhari)***

Ambapo hii ni hadith inayotuonesha katazo la Viapo vya Kijahiliya ambavyo ndani yake hua ni vyenye kuwataja Wazee wao waliokwishafariki. Na anasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri kua: Watu wenye Ilm wametofautiana kuhusiana na maana ya Kuharamishwa Kuapa kwa Vyengine zaidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Kwani Kuna Wasemao kua kulikokatazwa ni Kuapa kama walivyokua Wakiapa Watu wa Ujahilliyah Kuwatukuza wengine zaidi ya Allah kama vile Al Lat na al Uzza, na Mababu zao. Hivyo Mtu atakaepa kwa kupitia vitu kama hivyo hua anafanya Dhambi, ingawa hua haitajiki kutoa Kafara, lakini kuapa kwa kutumia vitu vyengine kwa mfano Mtu kuapa kwa utukufu wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Utukufu wa Uislam, Utukufu wa Ibada ya Hija, Utukufu wa Umra, wa Udhhiya,wa Sadaqah, wa Kuachia Huru Mtumwa n.k ambavyo ni Vitu vyenye utukufu wa Kumtukuza *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa nia ya Kumkaribia basi hua havijaingizwa kwenye haramisho.

Na miongoni mwa Wenye Mtizamo huo ni Ahu Ubayd na Wanazuoni wengine tuliokutana nao Ambao nao wamesimami kwenye maneno ya Masahaba *Radhi Allahu Anhum* ambao walikua Wakiwaapisha Watu kwa Kumuachia Huru Mtumwa, kwa Udhhiya na hata Sadaka mbali ya kua walikua wakijua kuhusiana na Katazo lililokuwepo.

Ambapo hii inamaanisha kua Hawakuwa ni wenye kujumuisha Katazo hilo kua ni la Jumla, kwa sababu kama ingekua ji la Kiujumla basi wasingewaapisha watu kwa Viapo hivyo.'(*Fat-h Al Barr)*

Hivyo kuhusiana na Kumtaja *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* au Vitu vyengine kwa ajili ya Kutoa Matumaini ya Uthibitisho juu ya kitu husika ambako hua si Kuapa, basi hua kumeruhusiwa kwa sababu amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua:

ما رواه أَبِو هُرَيْرَةَ رضى الله عنه قَالَ : جَاءَ رَجُلٌ إِلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم فَقَالَ : يَا رَسُولَ اللَّهِ أَيُّ الصَّدَقَةِ أَعْظَمُ أَجْرًا ؟ فَقَالَ صلى الله عليه وآله وسلم : أَمَا وَأَبِيكَ لَتُنَبَّأَنَّهْ؛ أَنْ تَصَدَّقَ وَأَنْتَ صَحِيحٌ شَحِيحٌ تَخْشَى الْفَقْرَ وَتَأْمُلُ الْبَقَاءَ،

Kuna Mtu alikuja kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na Kusema: Ya Rasul Allah Jee ni ipi Sadakah yenye Malipo bora zaid? *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Naapa Kwa Baba yenu, Bila ya shaka Mtajuulishwa, Mwambie kua Ni Kutoa Sadaqah Wakati Mtu akiwa na Afya yake, huku akiwa na akiwa anaogopa Umasikini, na huku akiwa anatamani abakiwe na Kitu katika Mali yake.'(*Bukhari na Muslim)*

Na amesema Imam Ahmad Ibn Hanbal kua:

وروي أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم أُتِيَ بِطَعَامٍ مِنْ خُبْزٍ وَلَحْمٍ فَقَالَ : « نَاوِلْنِي الذِّرَاعَ » فَنُوولَ ذِرَاعًا فَأَكَلَهَا ، ثُمَّ قَالَ : « نَاوِلْنِي الذِّرَاعَ » ، فَنُوولَ ذِرَاعًا فَأَكَلَهَا ، ثُمَّ قَالَ : « نَاوِلْنِي الذِّرَاعَ » ، فَقَالَ : يَا رَسُولَ اللَّهِ، إِنَّمَا هُمَا ذِرَاعَانِ ! فَقَالَ صلى الله عليه وسلم : «وَأَبِيكَ لَوْ سَكَتَّ مَا زِلْتُ أُنَاوَلُ مِنْهَا ذِرَاعًا مَا دَعَوْتُ بِهِ».

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alileletewa Chakula chenye Mjumuisho wa Mkate na Nyama. Hivyo akasema Nipe Mguu wa Mbele" nae akapewa Mguu wa mbele na akaula, na kisha akasema tena : Nipe Mguu wa Mbele, na akapewa na akaula, kisha akasema tena: Nipe Mguu wa mbele. Hivyo mmoja kati ya Watu akasema: *Ya Rasul Allah* Miguu ya Mbele hua ni miwili tu!**

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Naapa kwa Baba yako! Kama Ungekaa Kimya basi ingekua Unanipa Miguu ya Mbele tu, kwa kila wakati nnapohitajia.'(Musnad Imam Ahmad)*

Yaani Kama Sahaba huyo hakusema hivyo basi Miguu ya Mbele ingetokea tu kwenye Sahani Kimiujiza.

Naam..Hivyo anasema Shaykh Il Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Hii kusema Naapa kwa Baba wa Fulani hua si Kiapo bali ni Kauli ambazo zimo kwenye Utamaduni wa Kiarabu ambao umeingizwa bila kumaanisha kua ni Kiapo, Hivyo Katazo hua halihusiana na maneno haya bali hua Linahusiana na Viapo vya kweli kutokana na Kutukuza wanaoapiwa kwa kulinganishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***(*Al Majmuu)*

Ambapo kwa upande wa *Mujaddid Ad Din* Imam Ibn Hajar Al Asqallani basi Yeye anaendelea kusema kuhusiana na Kauli hizi kua: '**Anasema Imam Al Baydawi kua Hizi ni kauli ambazo hua zinatumika kwa ajili ya Makusudio ya Kutilia Mkazo au Kuthibitiaha kitu**. **Kwani Viapo hua havikusudiwi kwa Kauli kama hizi, kama vile ilivyokua Kauli za kawaida zinazotamkwa bila kukusudia Maana ya Kitu husik**a.'*(Fat-h Al Barr)*

Na anasema Mwanafunzi wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii ambae ni Imam Alaa Ad Din Ali Ibn Ibrahim Ibn Attar Al Dimashq Al Shafii kua: '**Mara**

kadhaa tunaona kua Viapo vinatajwa katika Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na vile tunaona Viapo katika Kitabu kitukufu cha *Allah Subhanah wa Ta'ala* Lakini Mtizamo wetu sisi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Viapo Visivyokubalika ni Kinyume na Viapo vinavyoapwa na mwengine zaidi ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo kwa upande wa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi yeye ni mwenye haki ya Kuapia kwa Ukubwa wa kiumbe chake chochote kwa ajili ya Kukumbushia Utukufu na Ukubwa wa Viumbe hivyo na Heshima na Unyenyekevu wao mbele yake. Kwa Mfano *Allah Subhanah wa Ta'ala* anaapa kwa kusema:

﴿وَالذَّارِيَاتِ ذَرْوًا﴾

Wa Aldhariyaati Dharwan* - Naapa kwa Upepo Unaopeperusha na Kutawanyisha(Surat Adh Dhariyyah 51:01)*

﴿وَٱلطُّورِ﴾

Wa Al Turi* -Naapa kwa Mlima Turi(Surat Tur 52:1)*

﴿وَٱلْمُرْسَلَٰتِ عُرْفًا﴾

Wa Almursalaati A'aurfan* - Naapa kwa Wajumbe (Malaika) Wanaotumwa kwa kufuatana mmoja baada ya mwengine.(Surat Mursalat 77:01)*

﴿وَٱلسَّمَآءِ وَٱلطَّارِقِ﴾

Wa Al Samaai Wa Tariq*- Naapa kwa Mbingu Na Nyote ya Usiku.(Surat Tariq 86:01)*

﴿ وَٱلَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ﴾

Wa Al Lalyli Idha Yaghshaa*- Naapa Kwa Usiku Unapofunika.'(Surat Layl 92:01)*

Na mithili ya Mifano kama hio Ambapo Viapo vyote hivi hua ni kwa ajili ya Kutilia Mkazo Utukufu wake *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Hivyo kuhusiana na Msimamo wetu basi ni kua Hairuhusiki kwetu sisi viumbe Kuapa isipokua kwa Kuapia kupitia kwake Muumba *Allah Subhanah wa Ta'ala, kwa* Kutumia Majina yake au Sifa zake ambazo hakuna anaeshirikiana nazo. Na hili limethibitishwa pale aliposema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Yeyote atakaeapa kwa zaidi ya Allah basi amefanya Shirk.

Imam Alaa Ad Din Ali Ibn Ibrahim Ibn Daud Ibn Attar Al Dimashq Al Shafii anaendelea kusema kua: '**Ama kuhusiana na Hadith isemayo kua Hivyo atakaeapa basi na Aape kwa Jina la Allah au akae Kimya, basi inamaanisha kua Kiapo kiwe ni kwa ajili ya Allah tu, hivyo atakaeapa na aape kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* au akae Kimya, na hivyo Amrisho la Hadith linamaanisha kua Bora Mtu akae Kimya, kwani vyenginevyo hua Imekatazwa.'*(****Khashiya Al Attari)***

Ambapo anasema Imam Abu Fadhl Zayn Al Din Abd Rahim Al Husayn Al Iraqi Al Shafii kua: ‘**Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Kuapia kwa Viumbe kua Imeharamishwa au Inakirihisha. Na Utofauti upo kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik na Imam Ahmad, ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik wanasema kua Inakirihisha, na kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Hanbal wanasema kua Ni Haram.**’

‘Hivi ndivyo wanavyosema wenyw Mtizamo wa Juu juu wa kimaana, na hii pia Kutokana na Mtizamo wa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ambae amesema kua: Kwangu mimi ni bora kuapia kwa Allah mara 100 na kisha nikapata Dhambi kuliko kuapia kwa zaidi yake na kisha nikatimiza kiapo.’

Ambapo kwa upande wa Imam Al Shafii basi amesema kua: Nnakhofia mimi Kuapa kwa mwengine zaidi ya Allah na kupata Dhambi.’

Ambapo As-hab wake Al Shafii wamesema kua Imekatazwa na ni Dhambi, hivyo Inaonekana kua wamesitasita juu ya jambo hilo ambapo Imam Al Haramayn amesema kua Madhhab yetu yana Uhakika kua Haikukatazwa (kama si kwa kukitukuza Kiumbe) bali ina kirihisha, na Imam An Nawawi amesema kua Inakirihisha katika Madhhab yetu kulingana na As-hab wetu lakini si haram kama ikiwa si kwa kukitukuza.

Wanazuoni wetu wanasema kua Kuapia kwa Kiumbe kwa njia ya Kukitukuza kama anavyotukuzwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi kunamfanya Mtu kutoka katika Uislam.’ *(Tarh Al Tathrib)*

Naam hio ni kuhusiana na Viapo vinavyoweza Kumtoa Mtu katika Imani ya Kiislam. Na kwa kua hili ni Jambo baya sana ambalo inabidi kila mmoja wetu kulijua au kua ufahamu mzuri juu yake basi na tuangalie mifano myengineyo, kwa kuangalia afueni inayoweza kupatikana juu ya Jambo hili kupitia katika maana ya meneno ya Aya ya Surat Al Baqara aya ya 286 isemayo kua:

﴿لاَ يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفْساً إِلاَّ وُسْعَهَا لَهَا مَا كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا ٱكْتَسَبَتْ رَبَّنَا لاَ تُؤَاخِذْنَا إِن نَّسِينَآ أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلاَ تَحْمِلْ عَلَيْنَآ إِصْراً كَمَا حَمَلْتَهُ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِنَا رَبَّنَا وَلاَ تُحَمِّلْنَا مَا لاَ طَاقَةَ لَنَا بِهِ وَٱعْفُ عَنَّا وَٱغْفِرْ لَنَا وَٱرْحَمْنَآ أَنتَ مَوْلاَنَا فَٱنْصُرْنَا عَلَى ٱلْقَوْمِ ٱلْكَافِرِينَ﴾

Laa yukalliful-laahu nafsan illaa wus’ahaa; lahaa maa kasabat wa ‘alaihaa maktasabat; Rabbanaa laa tu’aakhiznaaa in naseenaaa aw akhtaanaa; Rabbanaa wa laa tahmil-‘alainaaa isran kamaa hamaltahoo ‘alal-ladheena min qablinaa; Rabbanaa wa laa tuhammilnaa maa laa taaqata lanaa bih; wa’fu ‘annaa waghfir lanaa warhamnaa; Anta mawlaanaa fansurnaa ‘alal qawmil kaafireen *(Surat Al Baqara 2:286)*

Tafsir: **Allah haikalifishi Nafsi zaidi ya uwezo wake. Hupata malipo (kila Nafsi) kulingana na ilichokichuma na huaadhibiwa kulingana na ilichokichuma, Ewe Mola wetu usituadhibu kutokana na yale tuliyosahau au tuliyoyakosea Ewe Mola wetu usitubebeshe uzito kama ulivyowabebesha waliotangulia kabla yetu, Ewe Mola wetu Usitebebeshe zaidi ya tunavyoweza kustahamilia, Tufutie Madhambi yetu na Tusamehe, Tuingize kwenye Rehema zako kwani wewe ndie Mlezi wetu na tupe ushindi dhidhi ya makafiri.**

Hivyo hii ni aya yenye Dua ambayo inatupatia Afueni kutokana na Dhambi zinazofanywa bila Kukusudiwa, ikiweko kua na Ushawishi wa Kukufuru au kufanya Jambo la Kukufuru lakini bila ya Kukubaliana nalo ndani ya Moyo, Bila kuliamini, Kulisema au Kulifanya. Kwani anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* katika hadith ifuatayo kua:

أَخْبَرَنَا عُبَيْدُ اللَّهِ بْنُ سَعِيدٍ، قَالَ حَدَّثَنَا ابْنُ إِدْرِيسَ، عَنْ مِسْعَرٍ، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ زُرَارَةَ بْنِ أَوْفَى، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ تَجَاوَزَ لأُمَّتِي مَا وَسْوَسَتْ بِهِ وَحَدَّثَتْ بِهِ أَنْفُسَهَا مَا لَمْ تَعْمَلْ أَوْ تَتَكَلَّمْ بِهِ " .

Amesema Ubayd Allahi Ibn Said kua amesema Ibn Idrissa kua amesema Misaiyr kua amesema Qatadah kua amesema Abu Hurayrah kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* amaesamehe Ummah wangu kwa kila kitakachowajia Katika Ufahamu wao, na kisha ikawa hawakukifanya kitu hicho au hawakukisema' *(Sunnan An Nasai)*

Ambapo amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kuhusiana na Hadith hii kua: '**Kama Ikiwa Kuna Mawazo au Mtizamo ambao haujakaa Moyoni na Kudumu, basi hua ni wenye Kusamehewa kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni Na hii ni kwa sababu Mtu husika hua hana hiari na uwezo wa kuachana nayo Mawazo husika na hii ndio maana iliyokusudiwa na Hadith hii.**

Ambapo Wanazuoni wamesema kuhusiana na Mawazo yasiyodumo Moyoni, iwe Kusengenya, Kukufuru n.k. Hivyo kama Mtu akijiwa na mawazo ya Kukufuru bila ya kua na nia hio, na kisha akarudi haraka na kuachana na Mawazo hayo basi hua hajakufuru,na Hivyo hua hakuna wajibu wowote juu yake*(Al Adhkar)*

Na amesema Mujaddid Ad Din Shaykh Ul Islami Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**An Nawawi amesema kua Aya hii (Surat Al Baqara 2:286) ni Ushahidi tosha Mtizamo wa Skuli Madhhab ya yetu kua Watu wote watahesabiwa Matendo yao kutokana na kua na Mtizamo wenye Kudumu ndani ya Moyo. Ama kuhusiana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameusamehe Ummah wangu kutokana na Mawazo yao wakati wakiwa hawakuyasema au hakuyafanya, basi maana yake ni kua Kutokana na jua Mawazo hayo hayakuzama Moyoni na hivyo kuthibitishwa na kauli isemayo 'Au kuyafanya, kwa sababu Imani hua ndio Kitendo cha Moyo.'***(Fat-h Al Barr)*

Na akasema Imam Abdi Al Sindi Al Ansari Al Hanafi kua: **'Kuamini Kutokua na Imani Hua si katika Mawazo ya Kiroho, bali hua ni katika Matendo na kila kitendo Kulingana nacho, yaani Kauli iambatanayo na Kitendo husika iwe kitendo au Kauli, na hii ni kutokana na manenobya hadith yasemayo kua 'Pale itakapokua mtu huyo hakuyasema hayo,' basi hio haiwezi kua ni miongoni mwa sehemu mbili hizo**. **Bali hua ni Katika mtizamo wa Vitendo vya Mawazo ya Moyo tu lakini bila Matamshi.'***(Sharh Sunnah Ibn Majah, Sunnan An Nasai)*

Na miongoni mwa Hadith zinazozungumzia Mifano ya Irtiddad ni ile isemayo:

عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بنِ مَسْعُودٍ رضي الله عنه أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ:
سِبَابُ المسْلِمِ فُسُوقٌ، وَقِتَالُهُ كُفْرٌ

Amesema Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kumkashifu/Kumtukana Muislam hua ni Fusuq (Kufanya Maasi) na Kupigana nae Vita hua ni Kukufuru.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakrriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kuhusiana na Hadith hii kua: '**Ama Kuhusiana na Kupigana Vita na Muislam bila ya Sababu ya Haki basi hua haipelekei Muislam kutoka Katika Uislam na hii ni Kulingana na wengi Miongoni Mwa Wanazuoni,kwani Kufuru inayomtoa Mtu katika Imani hua ni kama Tulivyosema hapo kabla kua Mtu husika kua anaamini kua kupigana Vita Na Muislam mwenzake, hua inakubalika, ambapo Muislam hua akishaamini hivyo, basi hapa hua kuna Tafsiri kadhaa juu ya hili.**

Ambapo ya kwanza ni yenye kumhusu anaamini kua Inakubalika Kupigana vita na Muislam mwenzake bila sababu inayokubalika Kisharia.

Pili katika Kuamini kwake huko basi hua ni mwenye Kufanya Kufuru ya Ukarimu baina ya Waislam, kutooneana choyo kwa Neema baina ya Waislam,Kuvunja Udugu wa Kiislam, mambo ambayo japo hua si Kufuru ya kukosa Shukuran,lakini haya hupelekea Jambo la Tatu.

Jambo la tatu ni kuingia kwenye Kukufuru Kutokana na Uovu wake.

Jambo la nne ni kua Mambo haya yote hua ni sawa na kufanya Vitendo vya Makafiri na hivyo kumpelekea Mtu kufanana na Makafiri.' *(Sharh Sahih Muslim)*

Mfano mwengine ni kua anasema Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii kua : '**Ummah wa Kiislam unakubaliana kua Sharia za Dini ya Kiislam zimezibatilisha Sharia za Mitume wengine.'***(Al Mustasfa)*

Kwa Maana hio basi anasema Shaykh Ul Isami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: **'Muislam yeyote yule atakaekua haamini kua Mtu yeyote yule anaaefuata Dini isiyokua ya Kiislam kua Si Kafiri, au ana shaka ya kua watu hao ni Makafiri,basi Mtu huyo yeye mwenyewe hua ni Kafiri pia hata kama anaamini Imani ya Dini ya Kiislam.'(***Rawdat Talibin)*

Ambapo huu ndio pia Mtizamo wa Imam Ibn Abidin Al Hanafi katika Radd Al Mukhtar, Imam Ad Dardir Al Maliki katika *Sharh Al Shaghir,* na Imam Al Buhuti Al Hambali katika Kashaf Al Qina.

Na pia amesema Abu Dhar *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **'Hakuna Yeyoye yule atakaemshutumu mwenzake kwa Uovu au kwa Kukufuru isipokua Itamrudia yeye mwenyewe kama aliemsingizia hana hatia.'***(Sahih Bukhari)*

Na amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Muislam atakapomuita Muislam mwenzake kua ni Kafiri basi Ukafiri humrudia Mmoja wapo Miongoni mwao aliesingizwa au aliesingizia, au Ukafiri Utamrudia aliesingizia.'***(Muttafaq Alayhim)*

Hivyo Siku Moja Abu Sufyan *Radhi Allahu Anhu* alimuuliza Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kwa kusema: **Hivi Jee Umemtangazia Yeyote yule anaesali huku akiwa ameelekea Kibla cha Makkah kua ni Kafiri?'**

Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* akasema: 'La! Mua'adha Allah! -La Naomba Ulinzi kutoka kwa Allah Dhidi ya Hilo.'*(Mujam Al Awsat)*

Inasikitisha kua Irtiddad - Kutoka katika Uislam Imekua kawaida siku hizi pia kwa watu kutoana katika Uislam Unakuta Imam amepanda juu ya Mimbar katika Siku ya Ijumaa anatoa Khutba huku akiwaita Makafiri Waislam wenzake wanaoelekea Kibla ha Makkah Katika Ibada zao na kisha akishamaliza anashuka kwenye Mimbar na kusalisha Sala ya Ijumaa. Hivyo Jee kuna Ijumaa hapo? Tafakkar!

Hivyo mambo yatakayoweza Kumtoa Mtu katika Uislam yako mengi sana ambayo hata hivyo wengi wetu wakiwemo Maimamu wetu hua wanayaona kua ya Kawaida kiasi ya kua Wanawaita Waislam wenzao Makafiri kwenye Mimbar Kisha Wanasalisha Jumaa au Hadharani Mitandaoni yaani Ulimwengu wote Ujue. Na haya sio kama nasingizia La!..kwani yamejaa tele mtandaoni..*Subhanah Allah!*

Na anasema Imam Al Bayhaqi katika Sunan Al Kubra Kua: '**Nimemsikia mimi Abu Hazim Ibn Ahmad Al Abdawi Al Hafidh kua, Nimemsikia mimi Zahid Ahmafmd Al Sarkhasi akisema kua: Wakati kifo kilipomkaribia Imam Abu Hasan Al Ashari Jirani na Nyumba yangu Mjini Baghdad, basi aliniita Mimi na kuniambia:** '**Kua Shahidi Juu yangu kua Kamwe Sikuwahi mimi Kumuita Mtu hata Mmoja ambae anafanya Ibada kuelekea Kibla cha Makkah kua ni Kafiri Wakatofautiana sana na kuna ambao wameona kua inaruhusika kuiga kutoka kwa wengine kile ambacho itachukua mda mrefu kukielezea.'**

Haya yote ni mambo ya zamani sana tangu zama za Salaf Salih na waliofuatia baada yao, na sisi hatumjui Mtu yeyote Miongoni mwa Salaf wanaofuatwa wala miongoni mwa Tabiina anaefuatqa ambae amekataa Ushahidi wa yeyote yule alietofautiana nae kutokana na msingi wa Kitafsiri, hata kama Mtu huyo katafsiri sivyo na kukosea.''

Na tukiendelea na mifano ya Al Irtiddad basi anasema Imam Abu Bakr Uthman Ibn Muhammad Shatta Al Dimyati Al Shafii katika kitabu chake cha *Inayat Talibiin Aala Hal Alfadh Fat-h Muin* kua: '**Allah atunusuru Waislam sote na Watu wetu kutokana na Jambo hili**. **Irtiddad imegawika katika sehemu tatu ambazo ni Kimani, Kiviendo na Kimaneno.**

Aina ya kwanza ni Kua na Shaka juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Mitume wake, Vitabu vyake, Siku ya Malipo, Pepo na Moto Thawabu na Dhambi na kila kilichokubaliwa katika Dini ya Kiislam kua ni Wajibu, au Kuamini Kutokuwepo kwa Sifa za *Allah Subhanah wa Ta'ala,* au Kuruhusu Kilichoharamishwa.

Aina ya pili ni hua ni kama kwa mfano Kusujudia Sanamu, Jua, au Viumbe vyengine vyote.

Aina ya Tatu ni kusema au kumuambia Muislamu mwenzako: 'We Kafiri we!' au : 'Wewe Usiekua na Dini we.'

Na Hivyo kumaanisha Kuiskashifu Imani ya Dini yake anayoifuata ambayo ni Uislam kua ni Ukafiri. Na hapo kumaanisha Kumkashifu kwa Kutokana na Imani yake basi haiwezi kua Imani ya Dini ya Kiislam.

Au kwa Muislam kusema kua: "Kama Allah ataniadhibu mimi kutokana na Kutoweza kusali kutokana na Matatizo yangu au Maradhi yangu basi atakua amenikosea.'

Au kusema: 'Niyafanyayo si Kutokana na Majaaliwa ya Allah Juu yangu bali ni kutokana n uwezo wangu mwenyewe.'

Au kusema "Hata Kama Waislam wote watashuhudia Mbele yangu, basi Sitokubali" yaani kutokana na Kuwadharau Waislm.'

Au Kusema Baada ya Kutolewa Hukumu ya Kiislam kua: Hii Ndio Nini? Shariah? Na kupingana nayo na Kuikataa.

Au Kusema: 'Imeamrishwa Kuhudhuria katika Vikao vya Ilm, ndio Itaninufaisha nini Mimi Ilm ya Dini?'

Au Kusema: 'Laana ya Allah iwashukie Wanazuoni" na hivyo Kumaanisha Kuwadharau Warithi wa Mitume.'

Au Kusema: 'Sijwahi Mimi Kunufaika na chochote tangu nianze Kusali" Au "Kusema Sala ya Nini Mie?'

Au Mtu anaeumwa kwa Mda Mrefu kusema: 'Niwacheni Mimi iwe ni Muislam au Kafiri Sijali.'

Au Kusema: 'Mayahudi au Wakristo n.k ni bora Kuliko Waislam kwa sababu Wanasimamia haki za kadhaa w kadhaa."

Au Kusema: 'Mimi nakitaka Kitu hiki iwe cha Halali au cha Haramu.'*(Ianat Talibin)*

Imam Al Dimyati Al Shafii anaendelea kusema kua: **'Fahamuni kua Maneno mengi sana ya Kufuru hua yanazungumzwa na Watu wa Kawaida bila ya Wao kujua kua ni kufanya Al Irtiddad Hivyo ni Wajibu kwa wenye Kujua Kuyaelezea.'**

Na Imam Ibn Hajar Al Haytami ameelezea zaidi kuhusiana na aina zote za Irtiddad katika kitabu chake kiitwacho Al Ilam Bi Al Qawwathi Al Islam, Hivyo basi ataketaka kujua zaidi na akiangalie.'*(Ianat Talibin Aala Hali Al Fadh Ala Fat-h Al Muin)*

Kwani amesema pia Imam Taqi Ad Din Abu Bakr Ibn Muhammad Al Hasni Al Shafii kua: '**Irtiddad katika Shariah za Uislam hua ni Kutoka Dini ya Kiislam na kuingia kwenye Ukafiri na hivyo Kuukata Uislam.**

Hili ni Jambo ambalo baadhi ya Wakati hutokea kwa njia ya Maneno, kwa njia ya Vitendo na kwa njia ya Imani.

Na kila Moja kati ya haya mna mengi ndani yake Hivyo Tutataja kwa kifupi kwa kila aina kati ya hizi kama zinavyojulikana kwa njia nyengine.

Ama kuhusiana na Irtiddad ya Maneno basi hua ni: Kama Mtu akimkashifu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* au Kumdhihaki au Kumdharau basi Mtu huyo huhesabiwa kua ki Kafiri na hii mi Kuoingana na Makubaliano ya Wanazuoni.

Na kama Mtu Mtu akimwita Muislam Mwenzake kwa kusema "Ewe Kafiri!" Basi Moja kwa moja Mtu alieita huhesabika kua Yeye ni Kafiri, bila ya Kuangaliwa maana nyengjne yeyote ile ya Tafsiri ya maneno hayo, kwani hii hua ni sawa na Kuuita Uislam kua ni Ukafiri.

Ama kuhusiana na Irtiddad ya Kivitendo basi hua ni kama Kusujudia Masanam, Jua, Mwezi, nk. Pia Kuirusha Qur'an kwenye sehemu Chafu, Kufanya Uchawi n.k.

Na kama Mtu akifanya Kitendo ambacho Waislamu wanakubaliana kua ni chenye Kufanywa Kafiri, basi Mtu huyo hua amejitoa katika Uislam hata kama akisema kua yeye ni Muislam.

Ama kuhusiana na Irtiddad ya Kiimani basi hua ni yenye kusimamia kwenye Imani, Hivyo kama Mtu akiwa anaamini kua Umilele wa Ulimwengu, Umilele wa Viumbe wa *Allah Subhanah wa Ta'ala,* au haamini kuhusiana na Yale yaliyothibitishwa na Makubaliano ya Wanazuoni kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala,* au anathibitisha kile Kilichopingwa na Makubaliano ya Wanazuoni kuhusiana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi hua amejitoa katika Uislam Au yule anaeamini kua Kinaruhusika kile ambacho Wanazuoni wamekubaliana kua hakiruhusiki, au Kukana kile Kilichoruhusiwa na Makubaliano ya Wanazuoni, au Kuamini kitu kua ni Fardhi wakati kuna makubaliano ya Wanzuoni kua si Fardhi basi hua amejitoa katika Uislam.

Au Yule atakaamini kua si Fardhi Kile ambacho ni Fardhi kulingana na makubaliano ya Wanazuoni basi atakua amejitoa kwenye Uislam. Na Imam An Nawawi amesema katika Sifat Salat ndani ya *Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab* kua Yeyote atakaemfananisha, atakaemshabihisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi atakua amejitoa katika Uislam nami nasema pia kua Huo ndio Mtizamo sahih ambao hauepukiki kutokana na kua kufanya hivyo hua ni kupingana na maana halisi ya Aya za Qur'an.'(*Kifayat Al Akhyar Fii Hal Ghayat Al Ikhtisar)*

Ambapo anasema Imam Nazim Ad Din Al Balkhi Al Hanafi amesema kua: '**Kama Ikiwa Mtu mwenye hasira akiambiwa Hivi Humuogopi Mungu wewe?. Kisha nae akajibu La! Kwa hasira basi Mtu huyo hua tayari ameshajitoa katika Uislam'(***Fatawa Hindiyyah)*

Na akasema Imam Muhammad Ibn Ahmad Al Sarkhasi Al Hanafi kua: **'Kama Mtu akifanya Al Irtiddad, basi Ndoa yake hubatilika na Mke wake anatakiwa kutenganishwa ne iwe Mke huyo ni Muislam au ni wa Ahl Al Kitab, iwe ameshamuingilia ama la.'***(Al Mabsut)*

Na amesema Imam Mulla Al Qari Al Hanafi kua: '**Imam Al Shafii, Ahmad, Malik, Abu Hanifa, Al Ashar**i **Al Baqillani na Maimamu wote wa Mwanzoni na wa Baadae wa Uislam wanakubaliana kua Mtu anaemshabihisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua amejitoa katika Uislam na hafai Kusali Nyuma yake wala Kusaliwa.'***(Al Marqah)*

Na amesema Imam Ayyad Al Yahsabi Al Maliki kua: **'Yeyote atakaemkashifu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam, au* Kumkosoa,au Kumdhihaki, au Kumtia kasoro yeye au kizazi chake, au Wazee wake au Dini yake au Sifa zake, au Kumshusha Hadhi n.k Basi Wanazuoni wanakubaliana juu yake kua Mtu huyo amejitoa katika Uislam na anastahiki Adhabu za *Allah Subhanah wa Ta'ala.'***(*Al Shifaa)*

Na akasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Alish Al Maliki kua: '**Muislam yeyote yule atakaukashifu Uislam kwa Maneno iwe kwa kukusudia ama la basi hua ni mwenye kujitoa kwenye Uislam'***(Fatawa Alish Al Maliki)*

Na akasema Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: '**Kama Mtu akifanya Al Irtiddad basi Ndoa yake inabatilika na Mwanamke inambidi kukaa eda na hakuna ruhusa Kuingiliana wala kurudiana hadi Mhusika arudi kwenye Uislam, na kama hakurudi katika Uislam ndani ya Kipindi cha Eda basi ndoa hufutika bila Talaka.'***(Al Umm)*

Na amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: **'Na amesema Imam Al Shafii kua Kama Mtu akifanya Al Irtiddad basi anatakiwa atoe Shahada mbili (*Ashhadu An La Ilaha Illa Allah wa Ashhadu Anna Muhammada Rasul Allah*) Ambazo zitamtosheleza Kurudi kua Muislam, kwani Wanazuoni Wanakubaliana kua Shahada mbili hua ni Wajibu kwa Mhusika na hivyo Uislam hautorudi kwake bila Shahada mbili.'***(Rawdhah Talibin)*

Na amesema Mujaddid Ad Din Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na Toba ya Mwenye Kufanya Al Irtiddad hua ni Kuachana haraka na Irtiddad na Kushuhudia Shahada mbili yaani *Ashhadu An La Illaha Illa Allah wa Ashhadu Ana Muhammada Rasul Allah*, na kisha afanye Toba kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala.* Kwani Kutubu kabla ya Kushuhudia hua hakuna maana kwake na wala hakutomnufaisha, hivyo kwanza Shahad kisha Toba na juu ya hili kuna Makubaliano ya Wanzuoni.'***(Al Ijmaa)*

Hivyo Kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, Imam Ahmad Ibn Hanbal basi tunaona kua wao wanasema kua**: 'Al Irtiddad - Kutoka katika Uislam hua kunabatilisha Udhu, na pia hua Kunabatilisha Tayammam.'**

Na pia ndio Mtizamo wa Imam Al Awzai, Imam Abu Thawr Al Shafii na Imam Ibn Hazim Al Andalus. Hivyo kulingana na Mtizamo huu basi tunaona kua kama Mtu akifanya Al Irtiddad na kisha akarudi katika Uislam kwa Kutamka Shahada Mbili na Kutubu kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi kama atataka Kusali hua inambidi Kutia Udhu hata kama kabla ya Irtiddad yake alikua na Udhu.

Ambapo amesema Muwafaqa Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Allah atuepushe na Al Irtiddad, Kama Mtu akitia Udhu na kisha akasema Maneno ya Kufuru, kama Kumkashifu *Allah Subhanah wa Ta'ala* na kisha akatubu, basi hua ni Wajibu kwake kutia Udhu upya kwa sababu amali zake hua zimefutika, na hii hua ni kulingana na aya ya 65 ya Surat Az Zumar, na Udhu hua ni Amali.**

Hivyo na pia kama Mtu akiwa amefunga na kisha akasema Maneno ya Kufuru basi Funga yake hubatilika na itambidi ailipe.'*(Al Mughni)*

Ambapo amesema Imam Ibn Hazm kua: **'Ama kuhusiana na Al Irtiddad basi kama Mtu akitia Udhu, akikoga Janaba, akijitoharisha na Hedhi Na Kisha akatoka katika Uislam Bila ya Kujitengua Udhu na kisha baada ya Muda Mfupi akarudi katika Uislam, basi hakuna Aya wala Hadith wala Makubaliano ya Wanazuoni yanayothibitisha kua Kutoka katika Uislam hua ni Kunajisika kunakobatilisha Utohara.'***(Al Muhalla)*

Na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Al Shafii ni ule usemao kua: '**Kutoka Katika Uislam hakubatilishi Udhu kwa sababu Kinachobatilishwa na Al Irtiddad hua ni Malipo ya Amali husika na wala si Amali yenyewe husika.'**

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na Al Irtiddad - Kutoka katika Uislam na Udhu basi kuna Mitizamo Mitau tofauti juu yake.**

Ambapo Mtizamo wa Kwanza na Uliokua Sahih ni kua Kutoka Katika Uislam hua Kunabatilisha Tayammam lakini hakubatilishi Udhu.

Mtizamo wa pili ni kua Kutoka katika Uislam kunabatilisha Udhu na pia kunabatilisha Tayammam.

Na Mtizamo wa Tatu ni kua Kutoka katika Uislam hakubatilishi Udhu wala hakubatilishi Tayammam.

Na kuhusiana na Mtizamo wa kua Al Irtiddad inabatilisha Udhu basi huo ni Mtizamo ambao ni Dhaifu na hauna Nguvu.'*(Al Majmuu Sharh Muhadhdhab)*

Na amesema Imam Shams Ad Din Al Ramli Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Ibn Shihab Ad Din Al Ramli Al Shafii kua**: 'Ama kuhusiana na Kutoka katika Uislam hua hakubatilishi Udhu kwa sababu al Irtiddad hua haibatiliahi Vitendo hadi pale Itakapokua Mtu amefariki katika Hali hio'(***Al Mughni Al Muhtaj fii Sharh Al Minhaj)*

Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anaendelea kusema katika *Al Majmuu* kua: **'Kama ikiwa Mtu amekoga Janaba na kisha akafanya Al Irtiddad na kisha akarudi tena katika Uislam basi kulingana na Madhhab yetu ni kua Mtu husika Hatokua na Wajibu wa kukoga tena Upya Janaba, na bila ya Shaka kuna umuhimu wa Kukoga tena kama alivyosema Imam Al Rafii lakini hata hivyo si wengi waliokubaliana na mtizamo huo.**

Na kama ikiwa Mtu amefanya Al Irtiddad wakati akiwa anatia Udhu, na kisha hapo hapo akarudi katika Uislam, huku akiwa amefanya kitendo cha Udhu alipokua baina ya Kuingia na kutoka katika Uislam, basi kile alichokifanya katika wakati akiwa ametoka katika Uislam itabidi Akirudie baada ya kurudi katika Uislam ili Udhu wake ukubalike, kwani kile alichokifanya wakati akiwa katika haki ya Irtiddad hua hakikubaliki. Hivyo ndivyo alivyosema Imam Al Haramayn na Wanazuoni wetu wengineo.'*(Al Majmuu)*

Ama kuhusiana na Tayammam basi hubatilika kutokana na Al Irtiddad kwa sababu Nia hua ni Nguzo ya Tayammam ambayo hua inahitajika kwa ajili Kuomba Kuruhusika Kufanya Ibada ya Sala husika, hivyo Mtu aliefanya Irtidad hua amejibatilishia Nia ya Sala husika kutokana na Tayammam ya Sala husika.

Halafu pia kama tulivyoona hapo awali kuhusiana na Mtizamo wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na kua Tayammam hua haimtoharishi Mtu husika kutokana na Najis bali hua inampa ruhusa ya Kufanya Ibada husika, na hivyo Tayammam hua haimuingizi Mtu katika Utohara na kumtoa kwenye kukosa Tohara kama ilivyokua kwa Udhu.

Na pia Mtu atakaefanya Tayammam kwa kukosa maji basi kama akipata Maji tu hapo hapo Tayammam yake hubatilika, na hua haruhusiki Kusali bila Kutia Udhu au kujitoharisha kwa Maji, tofauti na mwenye kua na Udhu.

Hivyo Mwenye Kutayammam na kisha akafanya Irtiddad basi Tayammam yake hubatilika na kukosa ruhusa ya Ibada husika hata kama akirudi kwenye Uislam hapo hapo.

Naam..tufunge Mada yetu hii ya Al Irtiddad na Wudhu yaani Kujitoa Katika Uislam na Udhu kwa kuangalia suali linalohusiana na Kujitoa kwenye Uislam hua ni Kujiingiza Katika Najis na Hivyo Kunahitajia Kujitoharisha kwa Najis Kubwa kwa Kukoga Kogo la Janaba, ama la?

Na inabidi hili tuligusie kujua undani wake kwa sababu kuna Hadith isemayo kua: Amesema Qays Ibn Asim *Radhi Allahu Anhu* kua:

أتيت النبي صلى الله عليه وسلم أريد الإسلام فأمرني أن أغتسل بماء وسدر

‘**Nilienda mimi kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa nia ya Kuingia Kwenye Uislam, hivyo nae akaniamrisha Kukoga kwa kutumia Maji yaliyotiwa Majani ya Mkunazi.’**(*Sunnan Abu Daud, Imam At Tirmidhii na Imam An Nasai)*

Na kwanza kabla ya kuendelea basi tuwekeane wazi kuhusiana na Kujitohariaha kwa Kukoga kogo kama la Janaba, Ambapo anasema Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Al Baghawi Al Shafii kua**: ‘Inapendekezwa kwa Kila Muislam anaetaka kukutana na Watu au katika Tukio Muhimu kua Ajitoharishe kwa kogo la Janaba, kisha ajitie na manukato, na hii ikiwemo katika Siku ya Ijumaa, Siku za Idd mbili.**

Na Imam Al Muhamili Al Shafii amesema kua Inapendekezwa Kukoga Kogo la Janaba Kila baada ya Mtu kua ni mwenye kuingia kwenye hali ya Mabadiliko ya Kimaumbile Ikiwemo baada ya Jufanya Hijama, Baada ya Kuzimia na Kupata Fahamu, Baada Kuumwa n.k Kwa sababu Kukoga hua Kunatoharisha kila Kitu katika Mwili na kuurudisha Mwili katika hali yake ya Kimaumbile.’*(Al Majmuu)*

Na pia kuna Hadith isemayo kua: **‘Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua, amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaekosha Maiti basi na akoge Janaba baada yake.’***(Musnad Imam Ahmad, Imam Abu Daud, Imam At Tirmidhii)*

Ambapo hata hivyo anasema Imam An Nawawi kua: **‘Wanazuoni wa Madhhab yetu na wengi wa Madhhab mengineyo wanasema kua Kukoga Janaba naada ya kukosha Maiti hua Si Lazima, lakini hua inapendekezwa.**

Na amesema Imam Al Khattabi kua: Simjui mimi yeyote yule aliesema kua ni Wajibu; ila Ahmad Ibn Hanbal na Is-haq Ibn Rahawayh wamesema kua Kutia Udhu hua ni Lazima,lakini wengi miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua hua inapendekezwa. **Na hadith iliyozungumzia haya ni ya Abu Hurayrah ambayo Wanazuoni wanakubaliana kua ni Dhaifu.’***(Sharh Sahih Muslim)*

Naam sasa tunaporudi kwenye Hadith ya Qays *Radhi Allahu Anhu* aliyoamriwa Kukoga Janaba baada ya Kusilimu basi anasema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua**: ‘Kama mtu asiekua Muislam akaingia katika Uislam hua anawajibika kukoga Janaba, iwe Mtu huyo alikua Si Muislam wa Asili au Alietoka Katika Uislam na kisha akarudi tena katika Uislam, iwe alikua ameshakoga kabla ya Kuingia katika Uislam ama la, iwe alikua katika hali ya Janaba ama la.’***(Al Mughni)*

Ambapo huu ni Mtizamo wa Kwanza na pia ndio Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, Madhhab ya Imam Malik, Imam Abu Thawr Al Shafii, Imam Ibn Al Mundhiri Al Shafii na Imam Al Khattabi Al Shafii.

Ambapo kwa upande wa Imam An Nawawi basi anasema kuhusiana na Mtizamo huu kua: ‘**Kukoga Janaba hua Si Lazima, kwani tunapoangalia hadith basi tunatakiwa tuzichukulie kwa mtizamo wa kua zinaonesha kua Inapendekezwa Kukoga Janaba kutokana na kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuamrisha Qays kukoga kwa kutumia na Majani ya Mkunazi, wakati Kuna**

makubaliano Kukoga kua Kukoga kwa Kutumia na Majani ya Mkunazi hua si Lazima katika Janaba.

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* alikua anajua kua Qays alikua na Janaba na hivyo akamuamrisha Akoge kwa maji na Majani ya Mkunazi na wala si kwa sababu alikua amesilimu tu.'*(Al Majmuu)*

Mtizamo wa pili ambao ni Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab Ya Imam Abu Hanifa na pia Mtizamo wa Imam Abu Said Al Istikhari Al Shafii ambao wanasema kua: **'Kukoga Janaba Hua si Lazima kwa Mtu aliesilimu na kuingia kwenye Uislam, iwe mtu huyo alikua na Janaba ama la kabla ya kuslimu kwake.'**

Kwani anasema Imam Ibn Al Humam Al Hanafi kua: **'Kama Mtu asiekua Muislam ataingia kwenye Uislam wakati akiwa ni mwenye Janaba, basi hakuna kutokujubaliana juu yetu kua hakuna ulazima wa kukoga Janaba kwa sababu Janaba huondoka Baada ya Kuingia kwenye Uislam.'** *(Fath Al Qadir)*

Ambapo anasema Imam Al Mawardi Al Shafii kua: **'Kulingana na Mtizamo wa Abi Said Al Istikhari basi ni kua hua si Wajibu kwa sababu Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:**

﴿قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ إِن يَنتَهُواْ يُغۡفَرۡ لَهُم مَّا قَدۡ سَلَفَ وَإِنۡ يَعُودُواْ فَقَدۡ مَضَتۡ سُنَّةُ ٱلۡأَوَّلِينَ﴾

Qul lilladheena kafaroo in yantahoo yughfar lahum ma qad salafa wa-in yaAAoodoo faqad madat sunnatu al-awwaleena. *(Surat Al Anfal 8:38)*

Tafsir: **Waambie (Ewe Muhammad *Salallahu Alayhi wa Salam)* Wale ambao waliokufuru Kama Wakisita (Kukufuru) Basi Watasamehewa Yaliyopita, lakini kama wakirudia basi mfano tayari upppo juu ya wale waliotangulia.**

Na pia amesema Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Uislam Hufuta Yote yaliyotokea kabla yake.'*(Sahih Muslim)*

Na pia kama ingekua Kukoga Janaba ni Wajibu basi ingenukuliwa katika Hadith nyingi sana kutokana na Wingi wa Watu walioingia kwenye Uislam.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipomtuma Muadh Ibn Jabal katika Ardhi ya Yemen kuwaita katika Uislam, hakuambiwa kuhusiana na kuaamrisha kukoga Janaba.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Ambapo Imam An Nawawi Anasema kua**: 'Hadith Hio si hoja kwa sababu kuna Makubaliano kua Udhu hua ni Wajibu kwa Mtu aliesilimua na kisha akataka Kusali, hivyo hakuna tofauti kwa Mtu ambae amejisadia kisha akasilimu na Mtu mwenye Janaba na kisha akasilimu.**

Hivyo Hadith na Aya zinazungumzia kuhusiana na Dhambi tu, kwani kuna Makubaliano ya Wanazuoni kua Kama Mtu akiwa anadaiwa Pesa wakati akiwa Si Muislam basi hii haimaanishi kua na Deni hua limefutika kwa sababu amekua Muislam.' *(Al Majmuu)*

Kisha kuna Mtizamo wa Tatu ambao unasema kua: **'Mtu asiekua Muislam na akawa katika Hali ya kua na Janaba na kisha akasilimu basi hua ni Wajibu kwake Kukoga Janaba, lakini kama akiwa hayuko katika Hali ya Janaba basi hua si lazima bali hua inapendekezwa.'**

Ambapo huu ndio Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa pia. Kwani anasema Imam Ibn Hummal Al Hanafi kua**: 'Kukoga Janaba Kunapendekezwa Kwa yule Mtu ambae alikua si Muislam baada ya kuingia kwenye Uislam.'***(Fat-h Al Qadir)*

Na amesema Imam An Nawawi kua: **'Kama Asiekua Muislam atakua na Janaba au Hadath kubwa kabla ya kuingia kwenye Uislam basi Kukoga Janaba itakua ni Wajibu kwake baada Kusilimu, na huu ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii.**

Na kama ikiwa Ameingia Katika Uislam huku akiwa hana Janaba basi hua inapendekezwa kwake kukoga Janaba lakini hua hakuna ulazima kulingana na Mtizamo wetu. **Na hukmu hii hua ni sawa kwa Mtu ambae hakua Muislam, kwa Mtu aliefanya Irtiddad, aliekua akiishi na Waislam lakini si Muislam, au Mateka wa Kivita.'***(Al Majmuu)*

MUBTILAT SALAT – KUCHAKUA, KULA NA KUNYWA

❖❖❖❖

Baada ya Kuangalia na kukumbushana kuhusiana na Al Irtiddad na Udhu na Ibada ya Sala kukingana na Mitizamo ya Wanazuoni wa Madhhab Tofauti basi tunaingia katika kukumbushana juu ya Kuchakua, Kula na Kunywa wakati Mtu akiwa ndani ya Sala.

Na hili pia ni jambo ambalo Wanazuoni wamelizungumzia na bila ya Shaka kila walichokizungumzia basi hua pia ni Wajibu wetu Kukizungumzia, kwani kila kitu Kuhusiana na Ilm ya Dini ya Kiislam hua ni Muhimu Kukijua, hivyo amesema Imam Bukhari na Muslim kua:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رضي الله عنه أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ رَأَى نُخَامَةً فِي قِبْلَةِ الْمَسْجِدِ فَأَقْبَلَ عَلَى النَّاسِ فَقَالَ: مَا بَالُ أَحَدِكُمْ يَقُومُ مُسْتَقْبِلَ رَبِّهِ فَيَتَنَخَّعُ أَمَامَهُ؟ أَيُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَنْ يُسْتَقْبَلَ فَيُتَنَخَّعَ وَوَصَفَ فِي وَجْهِهِ؟ فَإِذَا تَنَخَّعَ أَحَدُكُمْ فَلْيَتَنَخَّعْ عَنْ يَسَارِهِ تَحْتَ قَدَمِهِ، فَإِنْ لَمْ يَجِدْ فَلْيَقُلْ هَكَذَا الْقَاسِمُ – أحد رواة الحديث – فَتَفَلَ فِي ثَوْبِهِ ثُمَّ مَسَحَ بَعْضَهُ عَلَى بَعْضٍ

Kwani anasema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **aliona Makohozi katika upande wa Kibla wa Msikiti.**

Hivyo akageuka kuwalekea Masahaba *Radhi Allahu Anhumu* na kisha akasema: Inakuaje Mtu mmoja miongoni mwenu anakua amesimama huku akiwa amemuelekea Mola wake na kisha anapiga Chafya Mbele ya Mola wake?

Hivi Jee yuko yeyote yule Miongoni mwenu ambae angependa kua Apigiwe Chafya na kutemewa Makohozi Mbele ya Uso wake. Hivyo kama mmoja wenu akipiga Chafya na ateme mate upande wa kushoto chini ya Mguu wake.**Na asipoweza basi na afanye hivi.'** *(Bukhari na Muslim)*

Ambapo Al Qasim mmoja kati ya Walionukuu Hadith hii anasema Kua: '***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akajitemea mate kwenye Nguo yake.'**

Na anasema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: **'Kama ingekua Mafua na Kohozi ni Najis basi isingeamrishwa kufutia kwenye Nguo katika wakati ambao Mtu anasali au Kutemea chini ya Mguu, na hakuna utofauti wa Utohara baina ya kile kinachotoka Kichwani na kinachotoka Kifuani.**

Na kuna Makohozi ya aina mbili yanayofanana hivyo kama ingekua ni Najis basi Mdomo ungekua na Najis Jambo ambalo hatujawahi kulisikia sisi kutoka kwa Masahaba.*'(Al Mughni)*

Na amesema Abu Said Al Khudry *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliona Kohozi kwenye Ukuta wa Msikitini. Hivyo akachukua Kokoto na kicha akalipangusa Kohozi hilo na kusema: Mmoja wenu atakapotema Mate basi asiteme mbele yake wala kuliani kwake bali ateme kushotoni kwake au Chini ya Mguu wake.'*(Sahih Muslim)*

Na imesemwa pia katika Mawsuah Fiqhiyyah kua**: 'Wengi Sana miongoni mwa Wanazuoni wanakubaliana kua Hairuhusiki Kutema Mate, Makohozi, Mafua kwenye Sehemu ya Sakafu ya Msikitini, au Ukutani mwake au kwenye Mabusati au Mazulia yake**. **Kwani Msikiti unatakiwa uhifadhiwe kutokana na Uchafu na Najis hata kama Uchafu husika utakua si Najis kama Mafua, Makohozi, n.k.'***(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaitiyyah)*

Ambapo anasema Mujaddid Ad Din Imam Ahmad Jbn Ali Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua**: 'Amesema Qadhi Iyad kua Kutema kitu katika Upande wa Kulia ndani ya Sala kumekatazwa pale inapokua kuna uwezekano wa Kufanya Vyenginevyo, hivyo kama ikiwa hakuna Njia nyengineyo basi inaruhusika.**

Lakini mimi nnasema kua hakuna Kutowezekan wakati Mtu husika anayo nguo aliyovaa, na Alieweka Sharia amesharuhusu kutemea juu yake
Na Al Khattabi amesema kua: Kama ikiwa kuna Mtu upande wa Kushoto yake Mtu, basi hairuhusiki Kutemea upande wowote isipokua chini ya Mguu wake au kwenye Nguo yake, yaani atemee Chini ya Mguu wake kisha na akanyage kupangusa.

Na Abd Razzaq amenukuu hivyo kutoka kwa Ataa kupitia kwa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*, hivyo kwa mfano kama ikiwa chini ya Miguu yake kumetandikwa Kitu na apangusie kwenye Nguo yake, na kama ikiwa hakuna cha kupangusia kama nguo, basi bila ya shaka Kuyameza itakua ni bora kwa mtu kuliko kufanya kilichokatazwa(ambacho ni Usiteme).'*(Fat-Al Barr)*

Hivyo juu ya hili la Kula, Kumeza Mafua au Makohozi hua inategemea na mazingira aliyokua nayo mtu, kwani kutokana na kua inakirihisha Kuyameza basi inaruhusika Kupangusa kwenye Nguo, Kitambaa au Tishu.

Na tumeanza kuangalia kuhusiana na vile vilivyomo na vitokanavyo ndani ya Koo na Mdomo wa Ibn Adam Kimaumbile kama Mafua, Makohozi, Mate, kua Inaruhusika Kutema au Kupenga katika Upande wa Kushoto kama tulivyoona katika Hadith ambayo kutokana nayo anasema *Mujtahid* Imam Al Qaffal Al Shahi Al Marwazi Al Shafii kua: '**Hadith inazungumzia Kuhusiana na kile Kitakachotoka Mdomoni au Kitakacho Juu ya sehemu ya Kichwani na Kushukia Mdomoni, ama kuhusiana na kile kitakachotoka Kutokea Ndani ya Kifua hua Si Tohara, na hakiruhusiki Kufukiwa Msikitini**.'*(Fat-h Al Barr)*

Hivyo anayoyazungumzia Imam Al Qaffal hapa kua hayaruhusiki Kufukiwa au Kupanguswa Msitiki ni Vitu kama Damu, Matapishi na vitu kama hivyo. Na tunapozungumzia vitu hivi basi hua tunazungumzia Vitu ambavyo hua ni Tofauti na Vyakula kwa sababu hua ni vyenye kutoka ndani ya Mwili wa Ibn Adam kupitia katika Viungo vya Mwili vinavyojumuisha Mfumo wa Chakula, na hivyo basi vitu hivi hua si Vyakula.

Na kutokana na kua Vitu hivi havijumuishwi katika Vyakula, basi tunaona kua kuna Kutofautiana kwa Wanazuoni Juu ya Mtizamo wa kua Kumeza kunabatilisha Sala ama la.

Kwani amesema Imam Al Hattabi Al Maliki katika Mawahib Al Jalil kua: '**Imam Al Lakhmi aliulizwa kuhusiana na Mtu atakaesafisha Koo yake, katika wakayi akiwa ndani ya Sala ambapo nae akajibu.**

Makohozi yeyote yatakayoenda Ndani Kooni na kisha Mtu husika akayameza basi hii hua haimbatilishii Funga yake wala Sala yake, hata kama ikiwa anaweza kuyatema, kama ikiwa hayajawahi kuzama Kooni - Ama kuhusiana na kama ikiwa yameingia Mdomoni mwake na kisha Na kisha akayarudiaha Ndani na kuyameza basi juu ya hili hua kuna Mitizamo miwili tofauti juu ya kua kua kama anatakiwa airudie Funga yake au Sala yake ama la.' *(Mawahib Al Jalil)*

Ambapo kwa upande wa Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Khatib Al Shirbini basi yeye anasema kua:**Miongoni mwa mambo yanayobatilisha Sala hua ni Kumeza Makohozi yanayokuja Kutokea Puani Kuingia Kooni pale Mtu anapokua na uwezo wa Kuyatoa, lakini akawa hakufanya Hivyo.'***(Al Iqna Fii Hal Al Fadh fii Matn Abi Shujaa)*

Na tunapoangalia zaidi kuhusiana na hili basi tunaona kua Wanazuoni wanajumuisha hukmu ya Tukio hili Kulingana na Ibada ya Funga na Sala kwa pamoja kama alivyofafanua Imam Al Hattabi kwa sababu anasema pia Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An NaWawi Al Shafii kua: '**Kama ikiwa Makohozi hayakufikia kwenye Kwenye sehemu ya Nje ya Mdomoni basi hua hayana Madhara, lakini kama ikiwa yanatokea Juu na kisha yakafikia Kooni basi hapa hua inahesabiwa kua kama ikiwa hakuwahi kuyatema na yakatumbukia hadi Tumboni basi hua hamna Tatizo, lakini kama akayarudisha yakiingia katika Uwazi wa Mdomoni na kisha akayameza baala ya kuyatema basi Funga yake hubatilika na hii ni kulingana na Mtizamo wa Madhhab yetu.'***(Al Majmuu Fi Sharh Muhadhdhab)*

Na hivyo kutokana na Fatwa hii, na Fatwa ya Imam Ibn Abi Shujaa kama ilivyofafanuliwa na Imam Al Shirbini basi hii inamaanisha kua kama ikiwa Makohozi yatawahi kuingia kwenye uwazi wa Mdomo wakati Mtu anasali na kisha nae akayameza basi itahesabika kua ameyala, na hivyo kama amefunga basi Funga yake ni Batili na kama anasali basi Sala yake Batili. Lakini kama ikiwa hayajawahi kuingia kwenye Uwazi wa Mdomoni bali yamepitia kooni moja kwa moja basi hii hua baina tatizo mbali ya kua ameyameza.

Hivyo Kumeza Makohozi, Mafua hua hakuhesabiki kua ni sawa na Kuyala na hivyo hakubatilishi Funga wala Sala pale inapokua hali hio imetokea katika Maeneo ya Hadd Al Batin (Maeneo ya Ndani ya Koo) bila kupitia katika Hadd Al Dhahir(Maeneo ya Nje ya Koo).

Ambapo inapozungumziwa Maeneo ya Ndani ya Koo hua ni Katika mipaka ya Maeneo yanayotoa sauti ya Herufi Haa Na herufi Hamza kuelekea ndani zaidi na inapozungumziwa maeneo ya Nje ya Koo hua ni katika Mipaka ya maeneo yanayotoa Sauti ya Herufi Kha kuelekea kutokea nje ya Mdomo.

Ama kuhusiana na mipaka ya maeneo ya sehemu za nje za Pua hua inamaanisha Kuanzia kwenye Tundu za Pua kuingia Ndani ya Pua.'*(Al Iqna Fi Hal Alfadh Abi Shujaa)*

Hivyo kama Mafua yakiwa katika Maeneo haya basi Wajibu hua ni kuyapenga au Kuyatema yakiiingia Mdomoni kama itawezekana kwani Kwani kama yakivutwa na akuingia Ndani Zaidi na kumezwa basi huhesabika kua Ni kuyala na hivyo Funga Hubatilika na Sala hubatilika.

Lakini kama ikiwa yameingia yenyewe labda kutokan na Kupiga Chafya, Kukohoa au kwa sababu yeyoye ile isiyodhibitika basi ha haina tatizo Ambapo huo ndio Mtizamo wa Madhhab Ya Imam Al Shafii, kama anavyosema Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmad Ibn Naqib Al Misri kua: 'Sala hua ni yenye kubatilika pale itakapokua hata kitu kidogo tu zaidi ya Mate kitakapoingia ndani ya Tundu za Uwazi wa mwili kwa Makusudi.

Na pia Sala hubatilika pale itakapokua kitu kimeingia ndani ya Mwili kutokana na Kutojalo kwa Mtu husika au Kutojua Hukmu yake kwa mtu husika pale itakapohesabika kua Kitu hicho kua si Kidogo bali ni Kingi.'*(Umdat Salik wa Uddat Nasik)*

Ambapo kwa upande wa Madhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Ali Shurunbulali Al Hanafi kua: '**Kumeza Majimaji, Mafua n.k yaliyofikia Mdomoni kutokea Puani hua hakuifanyi Funga ya Mtu kua ni Batili.'***(Maraqi Al Falah)*

Ama tunapozungumzia kuhusiana na kitu chenginecho kisichokua na asili ya kutoka ndani ya Mwili kama Mate, Mafua n.k na hivyo hua ni vyenye kuhesabiwa kua ni aidha chakula au kinywaji basi wanasema Wanazuoni kua Kumeza kitu chochote kwa kula au kunywa baada ya kuanza Ibada ya Sala hua kunabatilisha Sala, hata kama ikiwa ni kidogo.

Lakini kuhusiana na Kumeza kitu ambacho kilikua kimeganda kwenye Meno kwa sababu ya kua ni chenye kuliwa kabla ya kuanza Sala, basi hua hakubatilishi Sala, isipokua kama kitu hicho kitakua kikubwa na hii ni kulingana na Mtizamo wa Imam Al Awzai.

Lakini kuchakua kitu iwe kikubwa au Kidogo hua ni kwenye kubatilisha Sala, hata kama ikiwa Kitu hicho kilianzwa kuchakuliwa kabla ya kuanza Ibada ya Sala, na hii ni kwa sababu mambo yote haya hua ni Mjumuisho wa Mambo yanayofanywa nje ya Sala.

Na tunapoangalia Hadith za *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Sala na Kula basi tunaona kuna hadith isemayo kua: '**Amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua, amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

إِذَا وُضِعَ العَشَاءُ وَأُقِيمَتِ الصَّلاَةُ، فَابْدَءُوا بِالعَشَاءِ

Kitakapowekwa Chakula cha Usiku na kisha Ikaadhiniwa Adhana ya Sala ya Isha, basi Anzeni na Kula Chakula kwanza.'*(Sahih Bukhari)*

Na amesema Tena Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

إِذَا حَضَرَ الْعَشَاءُ، وَأُقِيمَتِ الصَّلَاةُ، فَابْدَءُوا بِالْعَشَاء

Kitakapowekwa Chakula kwa ajili ya Kuliwa na Sala Ikakimiwa basi Mtua anatakiwa Ale kwanza.'*(Sahih Muslim)*

Na akasema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua**: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

لَا صَلَاةَ بِحَضْرَةِ الطَّعَامِ، وَلَا هُوَ يُدَافِعُهُ الْأَخْبَثَانِ

Hakuna Sala (yenye kusalika Ipasavyo) pale inapokua Chakula Kiko Tayari au Mtu ameshikwa na Haja na anataka kuenda Chooni.'*(Sahih Muslim)*

Ambapo anasema Imam At Tirmidhii Katika Jamii At Tirmidhii kuhusiana na Hadith hizi kua: '**Hadith hizi zilikua zikifanyiwa kazi na Wanazuoni miongoni mwa Masahaba wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akiwemo Abu Bakr, Umar na Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum.* Na huu ndio poa Mtizamo wa Imam Ahmad na Imam Is-haq Ibn Rahawayh, ambao wote wamesema kua: 'Anza na Kula hata kama hii itakupelekea kuikosa Sala ya Jamaa.''**(*Jamii At Tirmidhii)*

Na amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Hadith hizi zinaonesha Uthibitisho wa kua ni Makruh kwa Mtu Kusali wakati Chakula alichokusudia kukila kikiwa tayari kimeshawekwa katika sehemu ya Kuliwa kwani Chakula hicho kitamtoa Mtu husika kutoka Utulivu wa Sala yake. Na pia hua ni Makruh kwa Mtu Kuzuia Mkojo au Mkorogo wa Ndani ya Tumbo lake.**

Inatakiwa ifahamike kua Kusali wakati chakula kiko tayari hua kunamuondolea Mtu Khushuu, hivyo Hukmu hii ya Kua ni Makruh kufanya Hivyo ni yenye kuendana na Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni wetu.'*(Minhaj Talibin)*

Na akasema Imam Al Qudamah Al Maqdisi kua: **'Chakula Kunapokua Tayari kimeshandaliaa basi hua ni Sunna kukila kabla ya Kusali, na Sababu ni kua Kufanua hivyo humuondolea Mtu mawazo juu ya Chakula na hivyo kumkosesha Mtu Khushuu, na Ni Sunnah kuharakisha kula Chakula cha Mchana au Jioni.'***(Mawsuah Al Fiqhiyyah Kuwaitiyyah)*

Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali amesema tena pia kua: **'Wanazuoni wetu wa Madhhab ya Imam Ahmad wamesema kua: Kwa hakika Kula kumepewa Kipaumbele zaidi kuliko Sala ya Jamaa pale itakapokua Mtu anahamu ya Chakula husika na Imam Al Shafii amekubaliana na Mtizamo wetu huu.'***(Mawsuah Fiqhiyyah Al Kuwaitiyah)*

Naam..hivyo tunapoangalia Hadith hizi na Fatwa zake basi tunaona kua zinatuwekea wazi kua Kula na Kusali hua ni vitu viwili tofauti na visivyoendana Kabisa, hivyo kila kimoja iinatakiwa kifanywe kwa kujitegemea, yaani kama Mtu unakula basi Unakula hadi Ukimaliza ndio Usali, na kama Unasali basi Sali hadi umalize kisha ndio Ule au Unywe.

Na Tunapozungumzia kuhusiana na Kula basi Tunazungumzia Kutia Kitu Mdomoni na kuanza Kukitafuna, Kukichakua na Kukimeza, au Kukimeza moja kwa moja kama ikiaa kitu hicho ni chenye asili ya maji yenye Kumimimika na hivyo kitendo hicho humaanisha Kunywa Na amesema Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu kua*:

أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ شَرِبَ لَبَنًا فَمَضْمَضَ وَقَالَ إِنَّ لَهُ دَسَمًا

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **alikunywa Maziwa, na kisha akaomba aletewe Maji na alipoleteaa basi akasukutua Mdomo wake na kusema: Maziwa ni yenye kuganda ganda Mdomoni.'***(Sahih Muslim)*

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi anasema kuhusiana na Hadith hii kua: '**Hadith hii inaashiria kua Inapendekezwa Kusukutua Mdomo baada ya Kunywa Maziwa Na Wanazuoni wanaifanyia kazi Hukumu iliyomo kwenye Hadith hii kua ni yenye kujumuisha juu ya Vyakula vya aina zote na Vinywaji vyote, kua Inapendekezwa Kusukutua, Kukosha Ndani ya Mdomo ili Ndani yake isibakie Dalili ya Chochote kile ambacho Kinaweza kikamezwa wakati Mtu akiwa anasali.'***(Sharh Sahih Muslim)*

Na ikasemwa kwenye Mawsuah Al Fiqhiyyah kua: '**Kusukutua hua kunapendekezwa baada ya Mtu kua ni mwenye Kula, kwani kuna Hadith ya Suwayd Ibn Nuaym** ***Radhi Allahu Anhu*** **ambae amesema kua:**

، قَالَ خَرَجْنَا مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم إِلَى خَيْبَرَ، فَلَمَّا كُنَّا بِالصَّهْبَاءِ . قَالَ يَحْيَى وَهْىَ مِنْ خَيْبَرَ عَلَى رَوْحَةٍ . دَعَا رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم بِطَعَامٍ، فَمَا أُتِيَ إِلاَّ بِسَوِيقٍ، فَلُكْنَاهُ فَأَكَلْنَا مِنْهُ، ثُمَّ دَعَا بِمَاءٍ فَمَضْمَضَ وَمَضْمَضْنَا، فَصَلَّى بِنَا الْمَغْرِبَ وَلَمْ يَتَوَضَّأْ. قَالَ سُفْيَانُ سَمِعْتُهُ مِنْهُ عَوْدًا وَبَدْءًا

Tulitoka Safarini pamoja na ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **katika Mwaka wa Khaybar Na walipofika katika maeneo ya As Sahba ambayo ni sehemu ya mwishoni mwa Khaybar,basi** ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akasalisha Sala ya Al Asr na kisha akaagizia Chakula kiletwe.**

Na hakikuletwa chakula chochote isipokua Sawiq ambacho ni Unga wa Shayiri au Ngano Iliyookwa Moto, hivyo ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akaamrisha kua Sawiq itiwe Maji kidogo kwa sababu ilikua Kavu sana.**

Na kisha yeye akala na sisi tukala, na kisha tukanyanyuka kwa ajili ya Kusali Sala ya Magharibi, na ***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*** **akasukutua na sisi pia Tukasukutua na kisha Akasalisha na hakutia Udhu.**

Hadith hii inatuonesha kua inapendekezwa Kusukutua baada ya Kula kabla ya Kusali, na Manufaa ya ya Kusukutua baada ya Kula Sawiq ambayo hata hivyo haigandi Mdomoni bali inaganda kwenye pacha za Meno au kwenye Pembe za Mdomo, na hivyo Kuzitoa hua kunaweza kumpelekea Mtu kumtoa katika Sala wakati Akisali.'*(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyah)*

Naam..imesemwa katika Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyyah kua: '**Wanasema Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal kua: 'Hua Ni Makruh kwa Mtu anaetaka Kusali Kutoa Kitu Mdomoni, hata kama kitu hicho hakitamzuia Mtu husika Kusoma au Kufanya Dhikr kwa sababu kitu hicho kitamtoa Mtu kwenye Kuijali Sala Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Anu Hanifa basi wao wamefafanua zaidi kwa kusema kua Kama kitu hicho hakitokua ni chenye kiyayuka Ndani ya Mdomo basi kitakua ni Makruh, lakini kama kikiwa ni chenye kuyayuka,basi kitambatilishia .tu husika Sala yake pale atakapokimeza baada ya Kuyayuka.**

Na kama Mtu kwa mfano akiweka Sukari Mdomoni, nayo ikayeyuka na kisha akaimeza kwa makusudi huku akiwa ni mwenye kujua kua kufanya hivyo hakuruhusiwi Au kwa sababu hakufuatilia juu ya jambo hilo Katika Sala, basi Sala ya Mtu huyo itabatilika.

Na pia Sala ya Mtu husika Itabatilika kama akichakua Kitu ndani ya Mdomo wake. **Hivyo kama Mtu akitokwa na kitu kulichoganda baina ya Meno yake kisha akakimeza, basi Sala yake Itabatilika***.'(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyyah)*

Ambapo amesema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: **'Kama mtu akimeza chakula Kilichoganda baina ya Meno basi Sala Yake haitobatilika**. **Lakini kama akila au akinywa kwa makusudi ndani ya Sala basi Sala itabatilika, na hii ni kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni miongoni mwa Wanazuoni wa Madhhab ya Hanbali.**

Na kama Mtu akila kwa makusudi hata katika Sala ya Sunnah basi Sala yake Itabatilika na hii ni Kuoingana na Mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Hanbali.

Na kama Mtu akila au Kunywa bila kukusudia iwe katika Sala ya Fardhi au Sala ya Sunnah basi Sala Haitobatilika na hii ni Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, na ndio Mtizamo wa Imam Ataa na pia Mtizamo wa Imam Al Shafii, kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua: 'Ummah wangu umesamehewa Kutokana na kukosea, kusahau na kutokana na Vitendo walivyolazimishwa kuvifanya.'

Na Imam Al Awzai amesema kua: 'Kama Mtu akila au akinywa bila kukijua katika Sala ya Faradhi basi Sala yake itabatilika na hii ni Kulingana na mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, kwa sababu Kula hua ni kitendo kirefu kinachojumuisha Kuchakua, Kutafuna Kumeza n.k hivyo bila ya shaka haiwezekani kwa Mtu kufanya hivyo bila kujijua ndani ya Sala.

Imam Al Awzai anaendelea kusema kua: 'Kama Ikiwa Mtu atameza chakula Kilichoganda baina ya Meno yake, na kam kikiwa ni kidogo hata kama kikiwa kinashindikizwa na Mate mengi basi Sala yake haitobatilika.''*(Al Mughni)*

Na anasema Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Ramli Al Shafii kua: **'Hukumu ya Ujumla ni kua Mtu anaposimama katika Sala mbele ya *Allah Subhanah wa Ta'ala,* basi hua anatakiwa kusimama kwa Unyenyekevu na Kujisalimisha kwa Mola wake na hivyo anatakiwa kujiweka mbali na kila kitakachopelekea kutaka kubatilisha Sala yake.**

Hivyo Mtu anatakiwa ahakikishe kua Mdomo wake uko Safi kabla ya Ibada ya Sala. **Hivyo tuseme kama Mtu atatia Peremende/Pipi Mdomoni Kwa makusudi huku akiwa anajua kua kula wala Kunywa hua hakuruhusiki katika Sala, na Peremende hio ni yenye sifa ya kuyayuka.**

Hivyo basi kama ikiyayuka katika wakati wa Sala yake, basi Sala yake itabatilika, lakini kama haikuyayuka basi Sala yake itakua Sahih na huu ndio Mtizamo unaotegemewa zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii.'*(Nihayat Al Muhtaj Al Sharh Al Minhaj)*

Na anasema Al Khatib Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shirbini Al Shafii kua: '**Kama Ikiwa kuna sehemu ndogo ya Chakula ndani ya mdomo wa Mtu anaesali basi Sala ya Mtu husika Hubatilika kwa sababu kitendo hicho hua ni chenye kuenda kinyume na Ibada ya Sala.**

Hii hua hivyo, isipokua pale itakapokua Mtu huyo amesahau au hajui Hukmu juu ya Jambo Kwa sababu ya kutokana na Kua yeye Ni Muislam Mpya ambae ndio kwanza amesilimu, au hajawahi kusomeshwa Juu ya jambo hili, ambapo kutokana na sababu hizi basi sehemu hio kidogo ya chakula haitoibatilisha Sala yake, na Allah ndie mwenye kujua Zaidi.'*(Al Mughni Al Muhtaj Ila Maarifat Al Maani Alfaz Sharh Minhaj)*

Kwa maana hio basi maneno ya Imam Al Khatib Al Shirbini yanamaanisha kua Kile kitakachopelekea kutobatilika kwa Sala ya Mtu aliesahau, Muislam Mpya au asiejua juu ya Hukumu hii basi ni Sehemu ndogo tu ya Chakula, kwa mfano kama kilichoganda kwenye Meno.

Lakini kama kikiwa ni kingi au kikiwa zaidi ya Punje ya Kunde au Mbaazi au Harage basi Sala itabatilika hata kama Mtu huyo kua ni Muislam mpya asiejua. Ambapo tunapozungumzia Hukmu hii basihua inamhusu kila Mtu iwe anaesali peke yake au Imam au Maamuma.

Hivyo kama ikiwa Maamuma atakua anajua kua Imam wake anasali na Peremende/Pipi Mdomoni tuseme basi kwanza Sala ya Imam hubatilika na Sala ya Maamuma pia kwa sababu ya kua ni mwenye kujua kua Imam wake hana Sala.

Na hivyo katika hali kama hii ya Maamuma kujua kua Imam wake ana Peremende Mdomoni basi Maamuma hua anayo haki ya Kukatisha Sala yake na kusali Peke yake.

Ambapo anasema *Shaykh Ul Islami* Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: **'Wanazuoni wetu wamesema kua: Kama ikiwa Mtu atakula au atakunywa kwa makusudi wakati akiwa ndani ya Sala basi Sala yake itabatilika, iwe kiliwacho ni kidogo au kingi,hili limewekwa wazi na Wanazuoni wetu. Na Msingi wa Hukumu hii ni kua kile kinachonatilisha Funga hua pia ni chenye kubatilisha Sala, na hivyo hakuna kutokukubaliana Miongoni mwa Wanazuoni wetu kua kufanya Hivyo hua kunabatilisha Funga pia.**

Imam Al Baghawi na wengineo wamesema kua Kuchakua tu peke yake hua kunabatilisha Sala, hata kama ikiwa hicho kinachochakuliwa hakiingii ndani na kufikia Tumboni yaani kama Ubani ambao hubatilsha Sala pia.

Na kama ikiwa kauweka tu Mdomoni bila kuutafuna na kisha ukaanza kuyeyuka kama ilivyo Sukari basi Sala hubatilika, na hii ni kutokana na Mtizamo unaokubalika zaidi Haya yote ni yenye kuhusiana na Kula kwa Makusidi.

Lakini kama ikiwa Mtu anakula kwa kusahau au hajui yaliyokatazwa ndani ya Sala, na anachokitafuna ni kidogo, basi Sala yake haitobatilika,na hii ni bila ya kutokukubaliana kwa Wanazuoni wetu juu yake. Lakini kama ikiwa kiliwachwo ni kingi basi Sala hubatilika na hii ni kutokana na Mtizamo mmoja wenye kuiubakika zaidi kati ya Mitizamo miwili.

Ama kuhusiana na wingi na Udogo wa Kitu husika basi hua ni kulingana na makisio ya vipimo vya Dasturi katika Jamii ya watu husika. Ama kuhusiana na Wanazuoni wengine basi Imam Ibn Al Mundhiri amesema kua: Wanazuoni wanakubaliana kua Hairuhusiki Kula wa Kunhwa kwa makusudi ndani ya Sala, na hivyo Mtu akila au Kunywa ndani ya Sala basi itambidi airudie Sala hio.

Ambapo kwa Upande wa Imam Ataa amesema Kua kama Mtu akifanya kwa kutojua basi Sala yake haitobatilika na mimi nasema hivyo hivyo.

Lakini kwa upande wa Al Awzai na Wanazuoni wanaofuata sana Kiyasi basi Wanasema kua Inabatilika. Ama kuhusiana na Sala ya Sunnah basi imeripotiwa kua Ibn Al Zubayr na Said Ibn Jubayr walikua wakinywa ndani ya Sala za Sunna.

Na Imam Tawus kasema kua hamna tatizo kufanya hivyo,lakini Imam Ibn Ak Mundhiri amesema kua Hivyo hua haituhusiki, hivyo huenda alieripoti hivyo alikosea.'*(Al Majmuu)*

MUBTILAT SALAT – KUCHAKUA, KULA NYAMA YA NGAMIA

❖❖❖❖

حَدَّثَنَا عُثْمَانُ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، حَدَّثَنَا أَبُو مُعَاوِيَةَ، حَدَّثَنَا الأَعْمَشُ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ الرَّازِيِّ، عَنْ عَبْدِ الرَّحْمَنِ بْنِ أَبِي لَيْلَى، عَنِ الْبَرَاءِ بْنِ عَازِبٍ، قَالَ سُئِلَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَنِ الْوُضُوءِ مِنْ لُحُومِ الإِبِلِ فَقَالَ " تَوَضَّئُوا مِنْهَا " . وَسُئِلَ عَنْ لُحُومِ الْغَنَمِ فَقَالَ " لاَ تَتَوَضَّئُوا مِنْهَا " . وَسُئِلَ عَنِ الصَّلاَةِ فِي مَبَارِكِ الإِبِلِ فَقَالَ " لاَ تُصَلُّوا فِي مَبَارِكِ الإِبِلِ فَإِنَّهَا مِنَ الشَّيَاطِينِ " . وَسُئِلَ عَنِ الصَّلاَةِ فِي مَرَابِضِ الْغَنَمِ فَقَالَ " صَلُّوا فِيهَا فَإِنَّهَا بَرَكَةٌ

Amesema Uthman Ibn Abi Shaybah, kua amesema Abu Mu'awiyah kua amesema, Al-A'mash kua amesema Abdullah Ibn Abdullah Al-Razi, kutoka kwa Abdul-Rahman Ibn Abi Layla, kua amesema Al-Bara' Ibn 'Azib *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa kuhusiana na Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia na akasema, Naam tia Udhu baada ya Kula nyama ya Ngamia.

Na akaulizwa kuhusiana na Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Kondoo ambapo nae akasema: Usitie Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia.'

Mtu huyo akauliza: Jee nnaweza kusali kwenye mazizi ya Ngamia?.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* akajibu kwa kusema: La!. Kwani kunatokana na Shaytani**

Mtu huyo akauliza tena kwa kusema: Jee nnaweza Kusali kwenye Mazizi ya Kondoo?.'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Naam kwani ndani yake kuna Baraka.'** *(Sunna At Tirmidhii, Sunan Abu Daud, Sunnan Ibn Majah)*

Na kuna hadith isemayo kua:

عن جابر بن سَمُرة، أن رجلاً سأل رسولَ الله – صلى الله عليه وسلم – أأتوضَّأُ من لحوم الغنم؟ قال: ((إن شئتَ فتوضَّأ، وإن شئتَ فلا توضَّأ))، قال أتوضَّأ من لحوم الإبل؟ قال: ((نعم فتوضأ من لحوم الإبل))، قال: أُصلِّي في مَرابضِ الغنم؟ قال: ((نعم))، قال: أُصلِّي في مَبَارِك الإبل؟ قال: ((لا

Amesema Jabir Ibn Samura *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Kuna Mtu alimuuliza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kwa kusema: 'Ya Rasul Allah* Jee ninatakiwa Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Kondoo?.'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Kama utataka basi Unaweza Kutia Udhu na Kama Utataka kutotia pia basi Usitie Mtu huyo akauliza tena kwa kusema Jee Nitie Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia?.'**

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Naam Tia Udhu baada ya kula Nyama ya Ngamia.'**

Mtu huyo akauliza tena kwa kusema: 'Jee nnaweza Kusali kwenye Mazizi ya Kondoo?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Naam'**

Mtu huyo akauliza: 'Jee nnaweza kusali kwenye mazizi ya Ngamia?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* akajibu kwa kusema: La!** *(Sahih Muslim)*

Ambapo Imam Ibn Khuzaymah amesema kuhusiana na Hadith hizi kua ni Hadith Sahih. Na huo ndio pia Mtizamo wa Imam Ibn Hibban, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imama Ibn Ajjarud na Imam Is-haq Ibn Rahawayh.

Na amesema tena Jabir Ibn Samura *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Hakika Sisi tulikua tukitia Udhu baada ya kula Nyama ya Ngamia, lakini hatukua tukitia Udhu baada ya kula Nyama ya Kondoo.**'*(Musannaf Imam Ibn Abi Shaybah)*

Na amesema Ummu Salamah *Radhi Allahu Anha* kua: '**Nyama ya Kuoka ya Kondoo iliwekwa mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* Hivyo akala sehemu ya Nyama hio na kisha akatoka na kuenda Kusali bila ya Kutia Udhu.**' (*Musnad Imam Ahmad, Sunan At Tirmidhii, Sunnan An Nasai)*

خرج رسولُ اللهِ صلَّى اللهُ عليهِ وسلَّم وأنا معهُ ، فدخل على امرأةٍ من الأنصارِ ، فذبحت له شاةً – ، فأكل منها ، وأتتْهُ بقناعٍ من رطبٍ فأكل منه ، ثم توضأَ للظهرِ وصلى ، ثم انصرف ، فأتتْهُ بعلالةٍ من علالةِ الشاةِ ، فأكل ، ثم صلَّى العصرَ ، ولم يتوضأ

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoka Pamoja nami, na aaingia kwa Mwanamke wa Kiansari ambae akamchinjjia Kondoo, na hivyo akala Nyama ya Kondoo huyo, na kisha aamletea mkebe wa Tende na akala pia Tende hio, na kisha akatia Udhu kwa ajili ya Sala ya Adhuhuri na**

kusali, na kisha akaondoka, na kurudi tene na Mwanamke huyo akamletea Mkebe wenye Nyama ya Kondoo nae akaila na kisha akasali Sala ya Al Asr bila ya kutia Udhu.

Na amesema Abd Allah Ibn Harith *Radhi Allahu Anhu* kua: '**Mikate na Nyama iliwekwa Mbele ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Wakati alipokua Msikitini, Hivyo akala sehemu ya Chakula hicho na Sisi pia tukala pamoja nae, Kisha Ikaadhiniwa Adhana ya Sala. Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akanyanyuka na Kusali, Nasi tukasali pamoja nae, huku sisi tukiwa hatuna sehemu ya Kujifutia isipokua kwenye Mchanga wa Msikitini.'***(Sunnan Ibn Majah, Imam Al Baghawi)***

Na anasema *Bahr Ul Ilm* Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

كان آخِرَ الأمرَيْنِ مِن رسولِ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم تَرْكُ الوضوءِ ممَّا مسَّتِ النَّارُ

'*Rasil Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikula Mguu wa Mbele wa Kondoo na kisha akasali bila Kutia Udhu Upya.'*(Muwwata Imam Malik, Sahih Bukhari na Muslim)***

Na kuna Hadith isemayo kua:

رَأَيْتُ رَسولَ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ يَحْتَزُّ مِن كَتِفِ شَاةٍ، فأكَلَ منها، فَدُعِيَ إلى الصَّلَاةِ، فَقَامَ وطَرَحَ السِّكِّينَ، وصَلَّى ولَمْ يَتَوَضَّأْ. قالَ ابنُ شِهَابٍ: وحدَّثَنِي عَلِيُّ بنُ عبدِ اللهِ بنِ عَبَّاسٍ، عن أبِيهِ عن رَسولِ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وسلَّمَ بذلك.

'Nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akikata sehemu ya Mguu wa Mbele wa Kondoo, na mara Adhana ikaadhiniwa, Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaweka Mguu huo wa Kondoo na Kisu chini na kisha akaenda Kusali bila kutia Udhu.' Anasema Ibn Shihab kua: 'Ali Ibn Abd Allah Ibn Abbas ameniambia mimi kua amesema haya baba yake kutokea kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam' *(Musnad Imam Ahmad, Sahih Bukhari na Muslim)*

Naam..hizi ni Miongoni mwa Hadith zinazothibitisha kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema kua Mtu akila Nyama ya Ngamia basi na Atie Udhu Upya, akila Nyama ya Kondoo basi hua hakuna ulazima wa Kutia Udhuu na pia zenye kuonesha kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alikula Nyama iliyopikwa bila ya Kutia Udhu tena Upya.

Na tumeanza nazo kwa sababu tunataka kufafanuliana kuhusiana na Mitizamo ya Wanazuoni Tofauti kuhusiana na Kula Nyama ya Ngamia na Udhu kua Jee Unabatilika ama la. Hivyo baada ya kuangalia Mifano Kadhaa ya Hadith kuhusiana na Kula Nyama ya Ngamia, Kula Nyama ya Kondoo, na Kula Nyama ikiyopikwa na Udhu basi tunaingia kwenye Mitizamo ya Wanazuoni kujua zaidi kuhusiana na na Udhu baada ya kula Nyama ya Ngamia kua kama unabatilika ama la.

Na hivyo tunapoangalia basi tunaona kua Wanazuoni wametofautiana juu yake jambo hili kwani iuna Wanaosema kua Udhu Unabatilika kutokana na Kula Nyama ya Ngamia na kuna wanaosema kua Udhu haubatiliki.

Ama kuhusian na wanaosema kua unabatilika ni pamoja na Sahaba Jabir Ibn Samura *Radhi Allahu Anhu,* Imam Muhammad Ibn Is-haq Ibm Yasar, Imam Abu Khaitham, Imam Yahya Ibn Yahya Al Nishapuri,Imam Abu Bakr Ibn Khuzaymah, Imam Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri, Imam Al Bayhaqi na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, n.k na wao wamesimamia kwenye Uthibitisho wa Hadith 2 za Mwanzo tulizoanza nazo Jana ambazo ni Hadith ya Jabir Ibn Samura na Baraa Ibn Azib *Radhi Allahu Anhum.*

Ambapo anasema Mujatahid Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Ibrahim Al Mundhiri Al Shafii kua: '**Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia hua ni Wajibu kutokana na Usahih wa Hadith hizi Mbili.'***(Al Awsat Fii Sunnan wa Al Ijmaa wa Ikhtilaf)*

Na miongoni mwa Wanaosema kua Udhu Haubatiliki kutokana na Kula Nyama ya Ngamia ni Abd Allah Jbn Masud, Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhum,* Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Malik na Wanazuoni wa Madhhab yake, Imam Abu Hanifa Nuuman Ibn Thabit na Wanazuoni wa Madhhab yake na Imam Muhammad Idris Al Shafii na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii.

Ambapo wao wanasimamia kwenye Uthibitisho wa Hadith ya Jabir Ibn Abd Allah ambae amesema kua:

كان آخِرَ الأمرَيْنِ مِن رسولِ اللهِ صلَّى اللهُ عليه وسلَّم تَرْكُ الوضوءِ ممَّا مسَّتِ النَّارُ

'**Moja kati ya Mambo ya Mwisho kufanywa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Kuachana na kutia Udhu baada ya Kula Nyama Iliyoguswa na Moto.**'*(Sahih Ibn Hibban, Sunna An Nasai,Sunna Abu Daud, Sahih Ibn Khuzaymah)*

Na anasema Imam Al Bayhaqi kua: **'Abd Allah Ibn Masud *Radhi Allahu Anhu* aliletewe Bakuli la Maini na Nundu ya Ngamia hivyo akala bila kutia Udhu baada yake.'***(Sunnan Al Kubra Imam Al Bayhaqi)*

Na Amesema Imam At Tirmidhii kua: '**Mtizamo wa Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia ni Mtizamo wa Imam Ahmad**.'*(Jamii At Tirmidhii)*

Na amesema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Imam Muhammad Idris Al Shafii amesema kua: Kama Hadith kuhusiana na Nyama ya Ngamia ni Sahih basi Nitaikubali.**'*(Talkhis Al Habir)*

Ambapo Maneno haya Ya Imam Al Shafii yanaoneaha kua Hadith hizi anazijua vizuri sana ila hajazikubali Usahih wake kutokana na Vithibitiaho vyake, kama vile ambavyo hazikukubakiwa na Imam Malik na Imam Abu Hanifa na Wanzuoni wao.

Kwani kuna baadhi wanaweza wakajiuliza : '**Hivi kwa nini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua Udhu unahitajika baada ya Kula Nyama ya Ngamia?'**

Ambapo mbali ya kua Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Hadith ya Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia, kwani kama tulivyoona kua Imam Al Shafii amesema kua kama Hadith hizo zingekua Sahih basi angezifuata.

Lakini pia kuna Wanazuoni wasemao kua Hadith hizo zimebatilishwa na Hadith ya Jabir Ibn Abd *Allah Radhi Allahu Anhu* isemayo kua Moja kati ya Mambo aliyoachana nayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Kuachana na Kutia Udhu baada ya Kula nyama Iliyoguswa na Moto.

Ambapo hata hivyo tukirudi Wanazuoni wa Madhhab Ya Imam Ahmad Ibn Hanbal wenye Kusimamia Mtizamo wa Kubatilika kwa Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia basi tunaona kua Imam Ali Ibn Sulayman Al Mardawi Al Hanbali anasema kua: '**Mtizamo Sahih ni kua baada ya Kula Nyama ya Ngamia Mtu hua anatakiwa Kutia Udhu, na Kutia Udhu ni kitendo cha Ibada, na huu ndio Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab yetu, na imesemwa kua Kuna Sababu Juu ya Amrisho la Kutia Udhu baada ya Kula Nyama ya Ngamia.'***(Al Insaaf)*

Na tunapoitafuta Sababu hio basi tunaona kua Imam Shams Ad Din Ibn Abd Allah Muhammad Ibn Abi Bakar Ibn Ayub Azur Ad Dimashq Ibn Al Qayyim Al Hanbali Anasema kua: '**Mtu anaekula Kitu basi hua ni mwenye kuambatana na Sifa za Kimaumbile za Kitu husika, kivitendo na kitabia. Kama vile ambavyo ilivyokua kwa *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Hikma zake za Kuumba kwake, basi hua kuna Hikma pia katika Maamrisho yake.**

Kwani *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekataza Kula Vitu visivyokua vya Halali na vichafu kwa sababu kama Mtu akivila vitu hivyo basi vitamuathiri kimaumbile na hivyo nae atakua kama kile alichokila Kwani Ibn Adam anapokula kitu hua ni sawa na kile alichokula, kwani hua kinaambatana nae ndani ya Mwili wake na hivyo hua ni sehemu ya Kitu husika.

Hivyo Ibn Adam kimaumbile amekua ni mwenye Kua katika hali ya katikati kitabia na kivitendo na hivyo kutofautiana na Wanyama wengine, kutokana na utofauti wa chakula cha Ibn Adam na Wanyama wengine.

Kwani Kula Damu na Nyama ya Wanyama wanaokula Nyama humfanya Ibn Adam kua na Maumbile ya Kimwitumwitu na Kishytani na Kikatili dhidi ya Ibn Adam wenzake. Hivyo Kihekima Sharia imekataza kuliwa kwa Vitu hivyo na Ibn Adam hadi pale itakapokua kuna Dharurah Kubwa sana itakayompelekea Kibn Adam kuruhusika kula Vitu hivyo.

Kama vile kwa sababu Wakristo wanakula Nguruwe basi Wamekua Ugumu na Ukatili wa Kimaumbile, ambapo hii hua ni sawa na Watu wanaokula Nyama ya Mbwa na Wanyama wengineo walao Nyama, hua nao wamechukua Tabia zao. Ambapo Tabia za Kishaytani Hua zinatokana na Wanyama wenye Meno Ya Kuchania Nyama, ambao wamekatazwa kuliwa kisharia.

Hivyo kutokana na kua Ngamia ni Mnyama mwenye kua na Sifa za Kikatili na Kishaytani, basi Uislam Umeamrisha kua Watakaokula Nyama yake wanatakiwa Watie Udhu ili kupingana na athari hizo za Ngamia za Kimaumbile.

Na kama vile ambavyo ilivyokua Punda ni mwenye Tabia za Kipunda Punda, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akakataza Kula Punda pia Na kutokana na kua Damu ndio kitu ambacho Shaytani hua anakitumia katika Kusafiria kwake ndani ya Miili yetu basi ndio pia *Allah Subhanah wa Ta'ala* akakataza Kuinywa.

Hivyo yeyote yule atakaetafakkari Maamrisho ya *Allah Subhanah ya Ta'ala* na Kuyazingatia basi atakua ni mwenye kujifungulia Mlango muhimu wa Ilm juu ya Ilm ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* na Sifa na Majina yae Matukufu.'*(Al Tibyan Fi Aqsami Al Qur'an)*

Na akasema tena Imam Ibn Al Qayyim kua: '**Nyama ya Ngamia hua inaathari kubwa katika mfumo wa hisia za Mwili kwa kuuongezea Nguvu zake na ndio Wanasayansi wakawaambia Watu wenye Hasira za karibu kua wasipendelee kula Nyama ya Ngamia Sana.**

Na Kutia Udhu kunatuliza Mfumo wa Hisia, ndio maana *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatuamrisha Sisi kutia Udhu pale tutakapopandwa na Hasira, ili tupate kupungukiwa na Hasira.'*(Ilam Al Muwaqqin Al Rabbi Al Alamin)*

Na amesema pia Imam Ibn Majah kua:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، حَدَّثَنَا هُشَيْمٌ، عَنْ يُونُسَ، عَنِ الْحَسَنِ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ مُغَفَّلٍ الْمُزَنِيِّ، قَالَ قَالَ النَّبِيُّ ـ صلى الله عليه وسلم ـ " صَلُّوا فِي مَرَابِضِ الْغَنَمِ وَلاَ تُصَلُّوا فِي أَعْطَانِ الإِبِلِ فَإِنَّهَا خُلِقَتْ مِنَ الشَّيَاطِينِ

Amesema Abu Bakr Ibn Abi Shaybah kua amesema Hushayma kua amesema Yunus kua amesema Hasan kua amesema Abd Allah Ibn Mughafal Al Muzani *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* kua: ''Salini kwenye Mazizi ya Kondoo lakini msisali kwenye Mazizi ya Ngamia kwa sababu Ngamia ameumbwa kutokana na Shaytani.'*(Sunnan Ibn Majah, Musnad Imam Ahmad)*

Ambapo anasema Imam Abu Sulayman Hamif Ibn Muhammad Ibn Ibrahim Al Khattab Al Busti Al Shafii kuhusiana na Hadith hii kua: **'Maana ya Hadith hii ni Kua Ngamia ana Maumbile ya Kama Shaytani pale anaposhtuka na kukasirika na hivyo anaweza kuibatilisha Sala ya Mtu husika.**

Na Waarabu hua ni wenye kuita kila asiekua na Usikivu kua ni Shaytani, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anamaanisha kua kama Mtu akiwa anasali karibu ya Ngamia basi kuna hatari dhidi yake pale Ngamia atakaposhtuka na huweza Kumpiga na Kumvamia anaesali katika Kukimbia kwao.'*(Maalim Sunnan)*

Ama tunaporudi kwa upande wa Kisayansi basi tunaona kua Nyama ya Ngamia ina mkusanyiko wa Maji kwa 78%, Protein na Amino Acids 19%, Mafuta 3%, Potassium, Phosphorous, Sodium, Calcium, Magnesiim, Zinc, Copper, Iron, n.k na hivyo kuifanya kua ni Nyama tofauti sana na Nyama za Wanyama wengineo Wanaoliwa kutokana na wingi zaidi wa Kiidadi wa Madini husika.

Nyama ya Ngamia ni yenye Manufaa mengi ikiwemo Kuzidisha Kinga ya Mwili Dhidi ya Maradhi ya Saratani, Presha, Mfumo wa Damu, Mfumo wa Hewa, Mfumo wa Uzazi,Mfumo wa Moyo na ukuaji wa Ubongo, Mifumo Muhimu ya Mwili na hivyo pia huongeza Joto la Ndani ya Mwili.

Naam..baada ya kuangalia Hadith tofauti juu ya Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ambao wao ni wenye kusema kua Kula Nyama ya Ngamia hua iunabatikisha Udhu, na kuangalia Sababu zao Kifiqh na Kisayansi kulingana na Utofauti wa Sifa ya Nyama ya Ngamia basi tunarudi kwa upande wa Wanazuoni wenye Mtizamo wa Kua Kula Nyama ya Ngamia hakubatilishi Udhu.

Na moja kwa Moja tunamkamata Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii ambae anatuambia kayika Sharh Sahih Muslim kua: '**Imam Muslim ametaja kuhusiana na Hadith zinazoelesea kuhusiana na Kutia Udhu baada ya kula Nyama iliyoguswa na Moto basi anafuatia baada yake kutaja kuhusiana na Hadith zinazozungumzia Kutotia Udhu baada ya kula Nyama iliyoguswa na Moto.**

Na hivyo kumaanisha kua Kutia Udhu baada ya Kula Nyama Iliyoguswa na Moto Kumebatilishwa. Na hii ndio Tabia ya Waislam na ya Wanazuoni wa Hadith, kwa kwanza kuanza na Hadith wanazozihesabu kua zimebatilishwa na kisha kufuatia Hadith zilizobatilisha hadith hizo.

Na Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na Hadith isemayo kua :

توضّؤوا ممّا مسّت النار

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua Tieni Udhu baada ya Kula Kilichoguswa na Moto.*(Sahih Muslim)*

Na hivyo Wanazuoni wengi wa Hadith wa Awali na wa baadae walikua na Mtizamo wa kua Udhu haubatiliki kutokana na Kula kile kilichoguswa na Motona Miongoni mwa wenye Mtizamo huu ni Abu Bakr Al Siddiq, Umar,Uthman, Ali, Ibn Masud, Abu Al Dardaa, Ibn Abbas, Ibn Umar, Nas, Jabir Ibn Samurah, Zayd Ibn Thabir, Abu Musa Al Ashari, Abu Hurayrah, Ubbay Ibn Kaab, Abu Talha, Amr Ibn Rabiah, Abu Ummamah, na Aisha *Radhi Allahu Anhum.*

Ambapo wote hao ni Masahaba, na wengi Miongoni mwa Waliofuatia baada yao Wana Mtizamo huu.

Na miongoni mwa Maimamu Wenye Mtizamo huu basi ni Imam Malik, Imam Abu Hanifa, Imam Al Shafii, Imam Ahmad, Imam Is-haq, Imam Abu Thawr na Imam Abu Khaytham.

Na pia kuna Wanazuoni wanaosema kua Udhu unabatilika baada ya Kula kile kilichoguswa na Moto na hivyo hua ni Wajibu kutia Udhu. **Na huu ni Mtizamo ulionukuliaa kutoka kwa Umar Ibn Abd Al Azizi, Hasan Al Basr, Al Zuhri, Abu Qilabah na Abu Majaz.**

Ambapo huku ni kutokukubaliana katika wakati wa kipindi cha zamani, na baada Wanazuoni wakakubaliana kua Udhu hauhitajiki kwa Kula kile Kilichoguswa na Moto, na Wanazuoni wengi wananukuu hadith zinazokataza Kutia Udhu baada ya Kula kilichoguswa na Moto, kua kama Urhibitisho, na Imam Muslim amezitaja Hadith nyingi sana humu na nyenginezo pia zimo kwenye Vitabu vyenginevyo vya Wanazuoni wa Hadith.'*(Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo anasema Mujjadid Ad Din Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii anasema kua: **'Imam Ibn Battal amesema kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliamrisha Kutia Udhu baada ya Kula Kilichoguswa na Moto kwa sababu Watu Walikua wamezoea kutokosha Vizuri Nyama katika Wakati wa Ujahiliyah, hivyo ikaamrishwa Kutia Udhu baada ya Kuila. Lakini baada ya Kuzoeleka kwa Usafi katika Uislam basi Amrisho hilo likabatilika.'***(Kitab Fath Al-Mun'im Sharh Sahih Muslim ,Fath al-Mulhim bi-Sharh Sahih al-Imam Muslim)*

Na tunapoangalia zaidi kuhusiana na Hadith zinazozungumzia Kula na Udhu, basi tunaona kua pia Kuna Hadith ambazo zimetumia Neno Wudhu Kilugha kumaanisha Kunawa Mikono na Mdomo tu.

Kwa mfano katika Sunnan Abu Daud na Sunnan At Tirmidhii katika Mlango wa Kunawa Kabla ya Kula na baada ya Kula isemayo kua: **'Amesema Qays Ibn Al Rabbi kua amesema Abu Hashim Al Rumani kua amesema Zadan kua:**

عن سلمان الفارسي ، رضي الله عنه قال قَرَأْتُ فِي التَّوْرَاةِ : أَنَّ بَرَكَةَ الطَّعَامِ الوُضُوءُ بَعْدَهُ فَذَكَرْتُ ذَلِكَ للنَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ ، فَأَخْبَرْتُهُ بِمَا قَرَأْتُ فِي التَّوْرَاةِ ، فَقَالَ رَسُولُ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَرَكَةُ الطَّعَامِ الوُضُوءُ

Amesema Salman Al Farsi *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘‘Nimesoma Mimi katika Taurat kua Baraka ya Chakula Imo katika Kutia Udhu baada ya Kula.’

Hivyo nikamwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salaam* kuhusiana na hayo niliyoyasoma kwenye Taurat, ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaniambia kua: Baraka ya Chakula imo katika Kutia Udhu kabla ya Kula na baada ya Kula.’’

Na kuna Hadith isemayo kua: ‘**Amesema Al Rubai Kua amesema Anas Ibn *Malik Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:**

.مَن أحَبَّ أنْ يُكثِرَ اللهُ خَيرَ بَيْتِه فلْيَتوضَّأْ إذا حَضَرَ غَداؤُه وإذا رُفِعَ

Yeyote yule anaetaka kua aongezewe Barka na *Allah Subhanah wa Ta'ala* Nyumbani kwake basi na Atawadhe pale Chakula chake kitakapokua Tayari Kula na pale atakapomaliza Kula.’*(Sunnan Ibn Majah, Imam Al Bayhaqi katika Shuab Al Iman)*

Na pia amesema Imam At Tabarani kua: **‘Udhu kabla ya Kula huondoa Umasikini.’**

Ambapo Mbali ya kua Hadith hizi ni Dhaifu kulingana na Vigezo vya Wanazuoni lakini hata hivyo ni Hadith ambazo zimetumia neno Udhu na Kutawadha kabla ya Kula na Baada ya Kula, ambako hua hakumaanishi kua ni Kutia Udhu wa Sala kabla ya Kula na Baada ya Kula bali kunamaanisha Kunawa Mikono na Mdomo.

Na kwa upande mwengine basi kuna Hadith isemayo kua:

أنَّ رسولَ اللَّهِ صلَّى اللهُ عليهِ وسلَّمَ خرجَ منَ الخلاءِ ، فقرِّبَ إليهِ طعامٌ فقالوا : ألا نأتيكَ بوَضُوءٍ ؟ فقالَ إنَّما أمرتُ بالوُضُوءِ إذا قمتُ إلى الصَّلاةِ

Amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitoka Chooni na kisha akaletewa Chakula, na kisha akaulizwa: ‘Jee tusikuletee Maji ya Kutia Udhu?.’

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: ‘Hakika mimi nimeamrishwa Kutia Udhu pale nitakapotaka Kusimamisha Sali.’(Sunnan An Nasai, Sahih Muslim)*

Ambapo Hadith hii pia imenukuliwa na Maimamu wengineo akiwemo Imam At Tirmidhii ambarme amesema kua: **‘Hii ni Hasan Hadith’** na pia Imam Al Bayhaqi ambae amesema kua: **‘Hii ni Hadith Sahih.’**

Na mbali ya Kutumika neno Udhu katika Kukosha Mikono lakini pia Hua kinatumika neno Ghusl yaani Kukosha. Kwa mfano kwenye Hadith ya Imam Al Zuhri isemayo kua: Amesema Abu Salama kua amesema *Aisha Radhi Allahu Anha* kua:

أن رسول الله صلى الله عليه وسلم كان إذا أراد أن ينام وهو جنب توضأ وضوءه للصلاة, وإذا أراد أن يأكل غسل يديه"

Alikua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Anapotaka Kulala huku akiwa na Janaba basi alikua akitia Udhu kama anaetaka Kusali na alipokua anataka Kula au Kunywa basi ali Ghusl Mikono yake kisha ndio Hula au Hunywa.'*(Musnad Imam Ahmad, Sunnan An Nasai, Sunnan Abu Daud)***

Na amesema Imam Imam Al Khallal kua: '**Amesema Muhanna kua nilimuuliza mimi Ahmad Ibn Hanbal kua nasikia Yahya Ibn Said amesema kua Sufyan hapendi Ku Ghusl Mikono kabla ya Kula? Hivyo kwanini hapendi?'**

Ahmad Ibn Hanbal akasema kua: Kwa sababu Ku Ghusl Mikono ni Dasturi ya Waajemi.'*(Kitab Shayib Al Iman)*

Hivyo hizo ni baadhi ya Hadith na Riwaya zinazoelezea matumizi ya Neno Udhu na Ghusl katika Kukosha Mikono na Mdomo katika wakati wa Kula. Ambapo matumizi ya Neno Udhu katika Hadithi hizi na Riwaya hua pia ni Vithibitisho vya Wanazuoni wenye Mtizamo wa kua Udhu haubatiliki kutokana na Kula Nyama ya Ngamia, ila Mtu hutakiwa Kukosha Mikono na Kusukutua Mdomo baada ya kula Nyama ya Ngamia kama ilivyosemwa katika *Tuhfah Al Alamii Sharh Jamii At Tirmidhii.*

Na kwa upande mwengine basi anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Abd Allah Al Khatib Al Tabrizi katika kitabu chake cha *Mishkat Al Masabih* kua: '**Anasema Ikrash *Radhi Allahu Anhu* kua Niliingia mimi Nyumbani kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na akanikaribisha Kula Chakula pamoja nae. Baada ya kumaliza Chakula *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaagizia Maji na kisha akanawa Mikono yake. Kisha akanigeukia mimi na kuniambia kua: 'Ewe Akrash Huu ndio Udhu unaotawadhwa baada ya kula kile Kilichoguswa na Moto.''***(Mishakat Masabih, Kitab Al Atimah)***

Na Aliulizwa Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Kutia Udhu baada ya Kula chakula Kilichopikwa hivyo akajibu:

لاَ، قَدْ كُنَّا زَمَانَ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لاَ نَجِدُ مِثْلَ ذَلِكَ مِنَ الطَّعَامِ إِلَّا قَلِيلًا. فَإِذَا نَحْنُ وَجَدْنَاهُ لَمْ يَكُنْ لَنَا مَنَادِيلُ إِلَّا أَكُفَّنَا وَسَوَاعِدَنَا وَأَقْدَامَنَا. ثُمَّ نُصَلِّي وَلاَ نَتَوَضَّأُ

La Hakuna Ulazima huo, na sisi ilikua hatuli sana Vyakula Hivyo katika wakati wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ila kwa Nadra. Hivyo kama tukipata Chakula kama hicho ilikua hatuna Vitambaa vya Kujifutia Mikono isipokua kujifutia Mikononi au Miguu mwetu, na kisha Tulikua Tukisali baada yake bila kutia Udhu.'*(Sahih Bukhari)*

Na Hivyo basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Muhyi Ad Din Imam Ahu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Udhu Haubatiliki kwa Kula Chakula Chochote, iwe Chakula hicho kimepikwa kwa Moto ama la, isipokua Kuhusiana na Nyama ya Ngamia ambayo Juu yake kuna Mitizamo Miwili**. **Na Mtizamo wa *Qawl Al Jaddid* (Mtizamo wa Kauli Mpya katika Madhhab ya Imam Al Shafii) na unaojulikana zaidi ambao ni kua Haibatilishi Udhu Na huu ndio Mtizamo sahih kulingana na Wanazuoni wetu, ambapo kulingana na *Al Qawl Al Qadim* (Mtizamo wa Zamani katika Madhhab ya Imam Al Shafii) usemao kua Unabatilika basi ni Mtizamo ambao usiokua na Nguvu miongoni mwa Wanazuoni wetu.'***(Al Majmuu)***

Na anasema Imam Ali Shurunbulali Al Hanafi kua: '**Ama Kuhusiana na kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoulizwa kuhusiana na Udhu baada ya Kula Nyama ya Kondoo na kisha akasema Tia Udhu baada yake Basi Udhu uliokusudiwa hapa na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Kukosha Mikono, kwa hakuna Hukumu ya Kubatilishika kwa Udhu katika Kula Nyama ya Ngamia, na hivyo Kukosha Mikono huko hua ni kutokana na Harufu nzito ya Nyama ya Ngamia.**

Ama kuhusiana na Mtizamo wa Wanazuoni wenye kusema kua Udhu hua unabatilika kwa Kula Nyama ya Ngamia Wametoa Hukumu ambayo ni yenye sifa ya *Ta'abbudi* (haikubaliki Kiakili) kama vile Kusali Rakaa Tatu kwa Salat Al Ishaa badala ya Nne.'*(Maraqi Al Falah)***.** Ambapo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Abu Muhammad Mahmud Ibn Ahmad Ibn Musa Badr Al Ayni Al Hanafi katika kitabu chake cha Sharh Abu Daud.

Na amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

إِنَّما الوُضوءُ ممّا يخرجُ وليسَ مما يدخلُ

Kwa Hakika Kubatilika kwa Udhu Hutokana na Kile kinachotoka Ndani ya Mwili na wala si kile kinacholiwa.'*(Imam Al Bayhaqi)*

Kwa kumalizia basi badhi ya Manufaa ya Ngamia ni kua: 'Amesema Imam Ibn Zuhayr kua: Manyoya ya Ngamia Yakichomwa kisha yakawekwa kwenye Jeraha linalotoa Dam, basi Damu hi itakata. **Na Nyama ya Ngamia Inaongeza Nguvu za Kujamiiana na kuondoa Uchovu baada kuingiliana.'***(Hayat Hayawan Al Kubra)*

Na amesema Imam Ibn Sinna kua: **Maziwa ya Ngamia huondoa Pumu**, **Kinyesi cha Ngamia Ukipaka huondoa Kovu, Chunjua, Vipele, Vidonda na Kuvimba kwa Viungo vya Miguu**. **Mkojo wa Ngamia huondoa Mba**. **Kujifukiza kwa Mafuta ya Nundu ya Ngamia huondoa Bawasili**. **Ubongo wa Ngamia ukichanganya na Siki hutibu Maradhi ya Kifafa**. **Mafuta ya Ngamia hutibu Maradhi ya Mshutuko wa Misuli ya Mwili.'***(Kanun Al Tibb)*

Na Imam Ibn Bakhtishu anasema kua: **'Ubongo wa Ngamia ukichemsha kwa Maji ya Mvua kisha ukinnywa huondoa Maumivu Mwilini. Nyama ya Ngamia hua ni Dawa ya Kuzuia Kuharisha.'**

Na Imam Ibn Jazla amesema kua: '**Korodani za Ngamia zikikaushwa na kusagwa kisha Unga wake ukichanganywa na Kinywaji hua ni Dawa ya alietafunwa na Nyoka.'**

MUBTILAT SALAT – NAJIS YA NGURUWE

❖❖❖❖

Kwani amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake Kitukufu kua:

﴿قُل لَّآ أَجِدُ فِي مَآ أُوحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلَىٰ طَاعِمٖ يَطۡعَمُهُۥٓ إِلَّآ أَن يَكُونَ مَيۡتَةً أَوۡ دَمٗا مَّسۡفُوحًا أَوۡ لَحۡمَ خِنزِيرٖ فَإِنَّهُۥ رِجۡسٌ أَوۡ فِسۡقًا أُهِلَّ لِغَيۡرِ ٱللَّهِ بِهِۦۚ فَمَنِ ٱضۡطُرَّ غَيۡرَ بَاغٖ وَلَا عَادٖ فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ﴾

Qul la ajidu feema oohiya ilayya muharraman AAala taAAimin yatAAamuhu illa an yakoona maytatan aw daman masfoohan aw lahma khinzeerin fa-innahu rijsun aw fisqan ohilla lighayri Allahi bihi famani idhturra ghayra baghin wala AAadin fa-inna rabbaka ghafoorun raheemun *(Surat Al Anaam 6:145)*

Tafsir: ***Sema Ewe (Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Sikupata kuona Mimi Katika Niliyoshushiwa Wahyi Kilichoharamishwa kuliwa Kwa anaetaka Kukila Isipokua Kama Itakua Ni Maiti(Nyama ya Mnyama aliekufa) au Damu Inayotiririka Au Nyama ya Nguruwe Kwani Kwa Hakika Hio, ni uchafu au Uasi wa Kidhambi wa Kilichochinjwa Kwa mwengine zaidi ya Allah Lakini Kama itamtokea Mtu Dharurah Bila Kutaka Kuasi au Kuvuka Mipaka basi Kwa Hakika Mola wako Ni Mwingi wa Kusamehe na Mwingi wa Huruma.***

Naam..hii ni Moja kati ya Aya zinazozungumzia Kuhusiana na Vile vilivyojaramishwa Kuliwa na Waislam kulingana na Maamrisho ya Muumba ambae ni *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Ambapo ndani yake Aya hii imetajwa Nyama ya Nguruwe.kama vile ilivyotajwa katika Aya nyenginezo mbili zinazofanana na aya hii kuhusiana na Vilivyoharamishwa kuliwa.

Na aya mbili hizo zenye kufanana na aya hii ni Aya ya Surat Al Baqara isemayo:

﴿إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيۡكُمُ ٱلۡمَيۡتَةَ وَٱلدَّمَ وَلَحۡمَ ٱلۡخِنزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ بِهِۦ لِغَيۡرِ ٱللَّهِ فَمَنِ ٱضۡطُرَّ غَيۡرَ بَاغٖ وَلَا عَادٖ فَلَآ إِثۡمَ عَلَيۡهِۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ﴾

Innamaharrama AAalaykumu almaytata waalddama walahma alkhinzeeri wama ohilla bihi lighayri Allahi famani idhturra ghayra baghin wala AAadin fala ithma AAalayhi inna Allaha ghafoorun raheemun*(Surat Al Baqara 2:173)*

Tafsir: ***Amekukatazeni Nyinyi Maiti, na Damu na Nyama ya Nguruwe na kile ambacho hakikuchinjwa*** **Kwa ajili ya *Allah Subhanah wa Ta'ala*. Lakini Yeyoye yule atakaekua na Dharura Na Akawa Hana Njia Nyengine isipokua kuasi (Kwa kula hivyo vilivyotajwa) Wala si kutokana na Matamanio basi kwa Hakika Mola wako Ni mwingi wa Usamehevu na ni Mwingi wa Huruma.**

Na aya ya Surat Al Maidah isemayo:

﴿حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ ٱلْمَيْتَةُ وَٱلْدَّمُ وَلَحْمُ ٱلْخِنْزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ لِغَيْرِ ٱللَّهِ بِهِ وَٱلْمُنْخَنِقَةُ وَٱلْمَوْقُوذَةُ وَٱلْمُتَرَدِّيَةُ وَٱلنَّطِيحَةُ وَمَآ أَكَلَ ٱلسَّبُعُ إِلاَّ مَا ذَكَّيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى ٱلنُّصُبِ وَأَنْ تَسْتَقْسِمُواْ بِٱلأَزْلاَمِ ذٰلِكُمْ فِسْقٌ ٱلْيَوْمَ يَئِسَ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ مِن دِينِكُمْ فَلاَ تَخْشَوْهُمْ وَٱخْشَوْنِ ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلإِسْلاَمَ دِيناً فَمَنِ ٱضْطُرَّ فِي مَخْمَصَةٍ غَيْرَ مُتَجَانِفٍ لإِثْمٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

Hurrimat AAalaykumu almaytatu waalddamu walahmu alkhinzeeri wama ohilla lighayri Allahi bihi waalmunkhaniqatu waalmawqoodhatu waalmutaraddiyatu waalnnateehatu wama akala alssabuAAu illa ma dhakkaytum wamadhubiha AAala alnnusubi waan tastaqsimoo bial-azlami dhalikum fisqun alyawma ya-isa alladheena kafaroo min deenikum fala takhshawhum waikhshawni alyawma akmaltu lakum deenakum waatmamtu AAalaykum niAAmatee waradheetu lakumu al-islama deenan famani idhturra fee makhmasatin ghayra mutajanifin li-ithmin fa-inna Allaha ghafoorun raheemun. *(Surat Al Maidah 5:3)*

Tafsir: **Mmeharamishiwa juu yenu Maiti na Damu na nyama ya Nguruwe na kile ambacho kimechinjwa si kwa ajili ya Allah, na kilichonyongwa au kupigwa kwa kipigo cha nguvu, au kwa kuangukia Kichwa, au kwa Kutobolewa na Pembe za Mnyama mwengine, na kile kilichobakia baada ya kuliwa na Wanyama wengine isipokua kama mtawahi kukichinja (kabla hakijafa). Na kile ambacho kimechinjwa kwa kutolewa kafara kwenye Madhabahu ya Masanam. Na pia kutumia mishare kwa ajili ya kutafuta bahati au kutoa maamuzi, yote hayo ni Uasi. Leo hii Wasioamini wote wameishiwa na matumaini juu ya Dini yenu, hivyo msiwe na khofu nao, bali kuweni na khofu nami. Leo hii nimeikamilisha Dini yenu, nimekamilisha fadhila zangu juu yenu na nimeuchagua Uislam kua ndio Dini yenu. Lakini kwa yule ambae atakumbana na Njaa kali (basi anaweza kula hivyo vilivyokatazwa), bila ya (kua ni mwenye) kuelemea kwenye dhambi, na kwa hakika Allah ni mwingi wa Kusamehe na ni mwingi wa Rehma.**

Na miongoni mwa Sababu za Kuharamishwa Kwa Nguruwe ni kutokana na kua na Maumbile ya Kua ni wenye Kula Nyama na Majani, wanakula Maiti na Vitu vilivyooza Wanakula hata maiti ya Ibn Adam na pia Kinyesi cha Ibn Adam na hata Kinyesi chao Wenyewe. Kwa maana hio basi bila ya Shaka kwa 1000% Nguruwe ni Wanyama ambao ni Wachafu na hivyo hua ni Najis.

Na Kimaumbile Nguruwe kutokana na kua ni wenye Kula kitu chochote kilichopo Mbele yao basi wamekua ni rahisi kwao kua ni Wabebaji wa Vijidudu, Virusi, Bakteria na Vimalea vya Maradhi tofauti ndani ya Miili yao na Nyama zao ambavyo huweza kusababisha Madhara ya Kiafya kwa Ibn Adam wakiwemo Minyoo ya aina ya *Lungworm na Tapeworms (Taenia Solium)* ambao wana uwezo wa kukua hadi kufikia urefu wa Mita 3 ndani ya Mwili wa Ibn Adam na Hutaga Mayai yao ndani ya Mwili ambayo huweza kusafiri mwili na kufikia kwenye Ubongo na Moyo.

Na pia wanabeba Minyoo ya aina ya *Spiral Trichinella* ambayo hua Haiivi wala Haiungui Ukiipika na hivyo Ukiwala wanaweza kusababisha Kupooza kwa Mwili na Muasho wa Ngozi. Nyama ya Nguruwe pia husababisha aina tofauti za Saratani ikiwemo Saratani ya Damu, Utumbo, Koo, Kizazi na ya Sehemu za Siri za Haja ndogo na kubwa.

Nyama ya Husababisha pia Maradhi ya Maumivu ya Viungo, Vidonda vya Tumbo, Figo, Mapafu, Maumivu makali ya Kichwa, Kukakamaa kwa viungo n.k. Naam..hizo ni baadhi ya sababu tu zilizopelekea Mnyama Nguruwe kua ni Najis na Kuharamishwa Kuliwa.

Hivyo kama tulivyoona katika aya tatu za Surah tofuati kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametuharamishia Kula Maiti, Nyama ya Nguruwe na pia Damu yenye kutiririka. Na tulizungumzia Kuhusiana na Damu Masfuuha pale tulipozungumzia Kisa cha Nabii Isa katika Kuwaelezea Mayahudi, hivyo kwa yule anaetaka kujua zaidi basi na atafute kitabu cha *Ulu ul Azmi Minna Rusul* Juzuu ya Pili cha *Al Mustakshif Abu Manal Danah* Ambacho kinapatikana bure Mtandaoni.

Hivyo tunapoangalia Aya zote tatu hizi ambazo ni za *Surat Al Baqara 2:173, Surat Al Maidah 5:3 na Surat Al AnAam 6:145* basi tunaona kua vitu vitatu vyote hivi vilivyoharamishwa ni kua Vina Madhara makubwa sana kwa Afya ya Ibn Adam.

Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* si mwenye kuwatakia shari Waja wake, kama alivyosema katika *Surat Al Aaraf* kuhusiana na Waja wake wale waliomuamini kua:

﴿ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلأُمِّيَّ ٱلَّذِى يَجِدُونَهُ مَكْتُوباً عِندَهُمْ فِى ٱلتَّوْرَاةِ وَٱلإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُم بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ ٱلْمُنْكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ ٱلْخَبَآئِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَٱلأَغْلاَلَ ٱلَّتِى كَانَتْ عَلَيْهِمْ فَٱلَّذِينَ آمَنُواْ بِهِ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيۤ أُنزِلَ مَعَهُ أُوْلَئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ﴾

Alladheena yattabiAAoona alrrasoola alnnabiyya al-ommiyya alladhee yajidoonahu maktooban AAindahum fee alttawrati waal-injeeli ya/muruhum bialmaAAroofi wayanhahum AAani almunkari wayuhillu lahumu alttayyibati wayuharrimu AAalayhimu alkhabaitha wayadaAAu AAanhum israhum waal-aghlala allatee kanat AAalayhim faalladheena amanoo bihi waAAazzaroohu wanasaroohu waittabaAAoo alnnoora alladhee onzila maAAahu ola-ika humu almuflihoona*(Surat Al Aaraf 7:157)*

Tafsir: **Wale ambao Ni wenye Kumfuata Mtume Nabii ambae Hajui Kusoma wala Kuandika Ambae wamemkuta Ameandikwa Ndani ya Tawrati (katika Deut xviii,15) na Injil (Katika Gospel John xiv 16) Akiwaamrisha Mema (Katika Kufuata Maamrisho ya Kiislam) na Kuwakataza Maovu Na Kuwahalalishia Vizuri na Kila Vya Halali Na Kuwaharamishia Vibaya na kila vya Haram na anawarahisishia kutokana na Uzito Na Kutokana na Minyororo waliyofungwa juu yao Hivyo Wale watakao Muamini *(Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam)* Wakamheshimu na Kumsaidia Na Wakaifuata Nuru (Ya Qur'an) Ambayo Ndio aliyoshushiwa Basi Wao ndio watakaokua Wamefuzu.**

Hivyo aya inatudhihirishia kua Kitabu akichokuja nacho *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yaani Qur'an iliyoshushwa kutokana na Rehma zake *Allah Subhanah wa Ta'ala* basi imeturahisishia kwa Kutuhalalishia Vitu Visafii vizuri vya Halali na Kutuharamishia Vitu Vichafu vibaya vya Haram.

Na bila ya shaka Nguruwe hajakatazwa katika Qur'an tu lakini pia amekatazwa katika Agano la kale ambalo linasema katika *(Leviticus 11:1-8)* kua : 'Na Nguruwe ni Wachafu Msile Nyama zao na wala Msiguse Mzoga yao.'

Maneno haya yamerudiwa pia katika *Deutronomy 14:8* Na pia katika Imani nyenginezo imekatazwa kula Nyama ya Nguruwe kwa mfano Wayahudi ambao hairuhusiki kwao Kula Nguruwe isipokua katika *Pikuach Nefesh* yaani pale itakapokua kuna hatari ya Uhai na hakuna

chakula chengine. Na historia inaonesha kua miongoni mwa watu waliokua hawali Nguruwe ni pamoja na Wagiriki wa zamani, watu wa Scotland wa zamani.n.k.

Naam, hivyo bila ya shaka *Allah Subhanah wa Ta'ala* amekataza Kuliwa Nguruwe kwa Hikma zake, na amemuumba kwa Hikma zake, kwani hakuna kitu alichokiumba kisichokua na maana na yeye ndie mwenye kukisimamia kikamilifu kila alichokiumba bila kuhijatia usaidizi wa aina yeyote.

Na anasema Imam Wahba Al Zuhayli Al Shafii kua: **'Haramisho la Mnyama aina ya Nguruwe linajumuisha kila Kitu chake kuanzia Ngozi, Mafuta n.k.'**

Ambapo *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameitaja Nyama Makhsusi kwa sababu ndio kitu ambacho ni chenye kukusudiwa zaidi kwa Wanyama kwani hua ni kwa ajili ya Kuliwa Hivyo Sharia imejumuisha sehemu zote za Mnyama Nguruwe na hii ni kutokana na maneno ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* yasemayo:

﴿أَوْ لَحْمَ خِنزِيرٍ فَإِنَّهُۥ رِجْسٌ﴾

Aw lahma khinzeerin fa-innahu rijsun. *(Surat Al Anaam 6:145)*

Tafsir: Au Nyama ya Nguruwe kwani kwa hakika Ni Chafu

Na pia amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua:

من لعب بالنردشير، فكأنما صبغ يده في لحم خنزير ودمه.

Yeyote yule atakaecheza Kamari hua ni sawa na aliezamisha Mkono wake Katika Nyama na Damu ya Nguruwe*(Sahih Muslim)*

Hivyo Kama ikiwa Kuigusa tu Nyama ya Nguruwe imekatazwa jee itakuaje kihusiana na Kuila, ndio itakua Imekatazwa kabisaa.'*(Tafsir Al Munir)*

Ambapo amesema Imam Ibrahim Al Baijuri Al Shafii kua: **'Wanyama wote waliokua hai ni Wasafi isipokua Mbwa na Nguruwe na kila watakachokizaa.'***(Hashiyah Al Baijuri)*

Na amesema Imam Ibn Rushd kua: '**Waislam aanakubaliana kuhusiana na Kuharamishwa kwa Khinziri na neno Khinziri hua linamaamisha aina zote za Nguruwe. Pale itakapokua aina ya Mnyama husika anajulikana kua ni Nguruwe Kijina, isipokua kama Mnyana anaitwa Nguruwe lakini si aina ya Nguruwe kwa mfano Nguruwe wa Majini.'***(Bidayah Al Mujtahid wa Nihayat Al Muqtasid)*

Lakini tunapoangalia kwa Upande wa Imam Ali Muhammad Ibn Habbib Al Mawardi Al Shafii basi yeye anasema kua: '**Ama kuhusiana na Mnyama mwenye Jina sawa na la Nguruwe lakini ni Tofauti na Nguruwe basi hua hajumuishiki kwenye Hukmu hii.**

Pale inapokua kuna Utofauti wa Mazingira ya Maisha yao, yaani kwa Mfano kama Punda na Punda Mwitu (Zebra) Ambapo ingawa wote ni Punda lakini Hukumu zao hua ni tofauti kwa

sababu Punda wa Mwituni anaruhusika Kuliwa lakini Punda wa Nyumbani hua haruhusiki kuliwa, mbali ya kua wote wanaishi Ardhini.

Hivyo Mnyama yeyote mwenye kutofautiana na mwegine kimazingira ya Kuishi yaani kama kuna anaeishi kwenye Maji na anaeishi kwenye Ardhi, basi hua inatakiwa Kutofautisha Hukumu zao hata kama wakiwa wana muonekano mmoja.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Ambapo katika Fatwa hizi tunaona kua Wanazuoni wametaja Nguruwe Maji na Kumtafautisha na Nguruwe wa Ardhini. Na hii ni kwa sababu Kuna Mnyama ambae kwa Kiswahili hua anaitwa Ngekewe lakini kwa Lugha ya Kiarabu hua anaitwa *Khinziri Al Maai.*

Ama kwa upande mwengine pia anasema Imam Kamal Ad Din Al Damiri kua: '**Aliulizwa Imam Malik siku Moja kuhusiana na Nguruwe wa Majini, kama ni halali ama la, ambapo nae akasema: 'Nyinyi Mnasema kua ni Nguruwe Maji Lakini Waarabu hua hawamuiti hivyo kwa sababu Waarabu hawajawahi kuona Nguruwe akiwa anaishi Majini, hivyo huyo Mnaemtaja nyinyi atakua ni Dolphin.'***(Hayat Hayawan Al Kubra)*

Ambapo Imam Wahba Al Zuhayli akasema kua: '**Nguruwe wa Majini hua ni Mnyama wa Majini na ambae hua hafanani na Samaki, lakini Sharia inasema kua Mnyama huyo ni Halali na hahitajii Kuchinjwa kama vile ilivyo kwa Samaki wa aina zote**.'*(Mutammad Fi Fiqh Imam Al Shafii)*

Kwani anasema Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakkalimin Imam Al Mushaqqiqin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Muhammad Ibn Umar Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kua: '**Kila Kitu kinachohesabika kua ni Kichafu kwa Maumbile ya Ibn Adam na chenye Kukirihisha kwa Ukinyaa wake Kwa Roho ya Ibn Adam basi hua ni Haram,kwa sababu vitu hivyo hua ni vyenye kusababisha Maradhi, na pia kutokana na kua kila kiinachosababisha Madhara hua na hukumu ya asili ya kua ni Haram.**

Hivyo kila kinachokirihisha kutokana na Ukinyaa wake basi hukumu yake ya asili hua ni kilichokatazwa, isipokua pale itakapokua juna Uthibitisho unaothibitisha kuruhusika kwake.'*(Mafatih Al Ghayb)*

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na Nguruwe basi ni Mnyama Mchafu na Ni Najis zaidi kuliko hata Mbwa, kwa sababu imeruhusika Kuwaua Nguruwe bila ya Kua na Sababu yeyote, na Kuharamishwa kwake kumedhihirishwa wazi. Hivyo kama Mbwa akiwa ni Najis basi Nguruwe ndio Najis zaid, ama kuhusiana na Kitakachozaliwa kutokana nao basi pia hua ni Najis kwa sababu ya kua Kimekua kimeumbwa kutokana na Najis.**

Na Imam Ibn Al Mundhiri amesema katika Kitabu chake cha Al Ijmaa kua Kuna Makubaliano ya Wanazuoni juu ya Nguruwe kua ni Najis, na huu ndio Uthibitisho uliokua na Nguvu zaidi kuutumia.
Lakini hata hivyo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanasema kua Nguruwe ni Tohara pale itakapokua yuko hai Ama kuhusiana na Uthibitisho wa Ibn Al Mundhiri ambao na wengine wameutumia pia basi hauna nguvu na sisi hatuna Uthibitisho wa wazi kua Nguruwe ni Najis.'*(Al Majmui Sharh Al Muhadhdhab)*

Naam..hivyo hapa tunaona kua Ingawa Wanazuoni wanakubakliana kua Nyama ya Nguruwe ni Najis na ni Haram kuliwa lakini kuna Utofauti wa Mtizamo juu ya Unajis wa Mnyama Nguruwe pale anapokua hajachinjwa, kwani Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wamepinga Unajis huo.

Kwa sababu anasema Mujtahid Imam wa Madhhab ya Imam Malik aitwae Muhammad Ibn Ali Ibn Umar Ibn Muhammad Al Tamimi Al Mazari al Maliki kua: '**Wanyama wote hai hua ni Tohara, na uthibitisho wa Haya ni wenye kutokana na Vithibitisho kadhaa ndani ya Qur'an na Sunnah ambavyo vinathibitisha kua Kila kitu hua ni Tohara hadi pale kitakapothibitishwa vyenginevyo.**

Hivyo bila ya shaka Nguruwe ameharamishwa Kuliwa, lakini hukumu ya kula Kitu hua ni tofauti na Na hukumu ya Utohara wa Kitu hicho pale kinapokua Hai. Hivyo katika Madhhab ya Imam Malik basi kila Mnyama aliekua hai hua ni Msingi wa Kwanini ni Tohara, hivyo pale Mnyama anapokua hai basi hua ni Tohara.

Na Mnyama Hua Najis pale anapokua anatiririkwa na Damu na pale anapokua ni Maiti.'*(Sharh Talqin)*

Na amesema Imam Al Khalili Ibn Is-haq Ibn Yaqub Al Maliki kua: **'Mtizamo unakubalika zaidi katika Madhhab yetu ya Maliki kuhusiana na Manyoya, Ngozi, Nywele ya Wanyama wote wanaoishi na Majasho, Machozi na Mate ya Wanyama wote hua ni Tohara, lakini Kama Nywele ikitolewa na Mzizi wake kutoka na Nyama basi mzizi huo utakua si Tohara kwa sababu umetoka na sehemu ya Mnyama.'** *(Mukhtasar Al Khalil)*

Kwa maana hio basi kwa Upande wa Madhhab ya Imam Malik tunaona kua Nguruwe aliekua hai na Manyoya yake, na Ngozi yake hua si Najis.

Naam..hivyo ingawa Nguruwe ameharamishwa Kuliwa kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameipa Nyama ya Nguruwe sifa ya Rijsun.

Ambapo neno Rijsun ni.lenye kutokama na neno Rajisa lenye kumaanisha Kunajisi, Kuchafua, Kufanya Dhambi, Kua Mchafu, Kua na Mtizamo wenye Shaka, Kuchukiza.
Hivyo neno Rijsi hua Linamaanisha Dhambi, Kitu ambacho kinastahiki Kuadhibiwa juu yake,Kitu ambacho hakina Kheri ndani yake,Kitu Kichafu, Kitukianchotokana na Uasi na Ushawishi wa Shaytan.

Hivyo kutokana na Nyama ya Nguruwe kupewa Sifa ya Rijsun basi wengi sana miongoni mwa Wanazuoni wanasema kua Nguruwe na kila kitu chake ni Najis iwe akiwa Mzima au Ameshakufa. Isipokua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik ambao mtizamo wao ni kama tulivyoona happ kabla.

Hivyo basi kulingana na Mtizamo huo tunaona kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik wanachukulia kua Risji ya Nguruwe ni ya Kisharia katika Katazo la Kuliwa kwake lakini si katika Hukumu ya Maumbile yake ya Nje. Na hii ni kwa sababu Neno Rijsi katika hali ya Najis limetumika mara kadhaa katika Qur'an kumaanisha Uchafu wa ndani ya Kitu na wala ai Uchafu wa Nje ya kitu yaani kwa mfano pale aliposema Allah Sunhanah wa Ta'ala kua

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡمُشۡرِكُونَ نَجَسٞ فَلَا يَقۡرَبُواْ ٱلۡمَسۡجِدَ ٱلۡحَرَامَ بَعۡدَ عَامِهِمۡ هَٰذَا وَإِنۡ خِفۡتُمۡ عَيۡلَةٗ فَسَوۡفَ يُغۡنِيكُمُ ٱللَّهُ مِن فَضۡلِهِۦٓ إِن شَآءَۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٞ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo innama almushrikoona najasun fala yaqraboo almasjida alharama baAAda AAamihim hadha wa-in khiftum AAaylatan fasawfa yughneekumu Allahu min fadhlihi in shaa inna Allaha AAaleemun hakeemun*(Surat At Tawbah 9:28)*

Tafsir: ***Enyi Wale Ambao Mmeamini Hakika ya Washirikina ni Najis Hivyo Wasiukaribie Masjid Al Haram baada ya Mwaka huu, na kama mtukua mnakhofia Umasikini basi Allah atakutajirisheni kutokana na fadhila zake, kwanikwa hakika Allah ni mwingi wa Hekima n ani mweenye kujua ju ya kila kitu.***

Ambapo Najis iliyozungumziwa hapa ya Washirikina ni Najis ya Ndani ya Nyoyo zao Kiimani, na Hivyo haimaanishi kua Miili yao ni Najis.

Na pia katika Surat Al Maidah pale iliposema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡخَمۡرُ وَٱلۡمَيۡسِرُ وَٱلۡأَنصَابُ وَٱلۡأَزۡلَٰمُ رِجۡسٞ مِّنۡ عَمَلِ ٱلشَّيۡطَٰنِ فَٱجۡتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

Ya Ayyuha Alladheena Amanoo Innama Walkhamru Waalmaysiru Waal-Ansabu Waal-Azlamu Rijsun Min AAamali Alshshaytani Faijtaniboohu laAAallakum Tuflihoona*(Surat Al Maidah 5:90)*

*Tafsir****: Enyi Mlioamini! Hakika ya Pombe, Kamari na Al Ansab na Al Azlamu (Mishale ya kuagulia na kubashiria na vyano vya kafara) ni uchafu miongoni mwa Amali za Shaytani, hivyo ziepukeni ili mpate kua ni wenye kufuzu.***

Ambapo Aya hii imejumuisha Vitu vya Kuchezea Bahati Nasibu na kuagua na kubashiria Kama Mishale ambayo watu wa zamami walikua wakitumia, na hivyo basi kumaanisha kua zana hizo zenyewe kama zana basi ni Halali, na hazijaharamishwa kilichoharamishwa ni Matumizi yake pale vitakapotumiwa sivyo.
Hivyo kutokana na kua Aya hazikuweka wazi Rijs ya Nguruwe bali imeweka wazi Rijs ya Nyama yake, basi ndio tunaona sasa kua Wanazuoni wametofautiana juu yake kiasi ya kua Baadhi ndio wakaamua Kukisia kiasi cha kua Unajisi wa Nguruwe na Unajis wa Mbwa Lakini wakasema kua Nguruwe ni Najis zaidi kuliko hata Mbwa na ndio maana tunaona kua Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii akasema kua:

ليس لنا دليل واضح على نجاسة الخنزير في حياته

بل مقتضى الدليل طهارته كالأسد والذئب والفأرة ونحوها

‘**Sisi Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii Hatuna Uthibitisho wowote uoneshao kua Nguruwe kama Nguruwe ni Najis anapokua Hai. Na hivyo anaweza akawa si Najis kama alivyo Simba, Mbwa Mwitu au Panya.**

Ila Ibn Al Mundhiri amenukuu juu ya Makubaliano ya Wanzuoni juu ya Unajis wa Nguruwe, ambapo hata hivyo makubaliano haya yana utata kwa sababu Imam Malik hakukubali yeye na amesema kua Nguruwe Si Najsi.

Hivyo Sisi Tunahitimisha kua Kula Nguruwe ni Haram, ama kuhusiana na Unajis wao basi Wanazuoni wengi Wanasema kua Ngurue ni Najis, na baadhi wanasema kua si Najis bali ni kama Punda na Mbwa Mwitu ambao ni Haram kuwala lakini si Najis.’*(Al Majmuu Sharh Al Muhadhhab)*

Kwani anasema pia Mujaddid Ad Din Sultan Al Mutakalimin Imam Al Mushaqqiqin Imam Al Ghazali Al Thani Imam Muhammad Ibn Umar Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii kua: '**Ama kuhusiana na Nguruwe basi Ummah Unakubaliana kua Kila kitu chake kimeharamishwa na *Allah Subhanah wa Ta'ala* ametaja Nyama yake kwa sababu Nyama ndio kitu Muhimu Zaidi**. **Yaani kama vile alivyosema Katika Surat Al Jumuah kua:**

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِن يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ﴾

Ya ayyuha alladheena amanoo idha noodiya lilssalati min yawmi aljumuAAati faisAAaw ila dhikri Allahi wadharoo albayAAa dhalikum khayrun lakum in kuntum taAAlamoona; *(Surat Al Jumuah 62:9)*

Tafsir: **Enyi Wale ambao Mmeamini Itakaponadiwa Sala Katika Siku Ya Ijumaa Basi Kimbilieni Utajo wa Allah Na Acheni Biashara Kwani Kufanya Hivyo ni kheri kwenu Kama Mngekua Mnajua.**

Hivyo haramisho la Nyama ya Nguruwe ni kutokana na Umuhimu wa Nyama ya Nguruwe zaidi kuliko kitu chengine chochote kama vile ilivyo kwa Wanyama wengine. Ambapo Umuhimu huo ni kama vile ilivyotajwa Biashara katika Aya hii ya *Surat Al Jumaah* kwa sababu Biashara ilikua ndio kitu Muhimu zaidi ya Shughuli nyenginezo.*(Mafatih Al Ghayb)*

Yaani Imam Fakhr Ad Din Al Razi anatukumbusha katika Asbab Nuzul ya Aya 3 za Mwisho za Surat Jumuah ambazo ni aya ya 9-11. Ambapo Tarikh zinaonesha kua hapo awali Sala ya Ijumaa ilikua ni kama Sala ya Idd mbili, yaani kwanza inasaliwa Sala na kisha ndio Inasomwa Khutba.

Kama anavyosema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua anatoa Khutba ya Ijumaa Madina, wakati Msafara wa Biashara kutoka Syria ulipoingia katika Mji wa Madina.

Na hivyo kwa haraka sama Masahaba wote wakatoka nje ya Msikiti kwa ajili ya kuupokea Msafara huo Hivyo ndani ya Msikiti walibakia Masahaba 12 tu waliokua wakisikiliza Khutba ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Hivyo ingawa aya imetaja Biashara kwa sababu ya Umuhimu wake kwa Waislam wa Madina katika Wakati huo lakini hata hivyo Aya inajumuisha kila aina ya Shughuli iwe Kulima, Kuvua, Kutenga n.k. Hivyo baada ya Amrisho la Aya basi ndio Mfumo wa Sala ya Ijumaa ukabadilishwa, kwa Khutba kuwekwa mwanzo. Kisha ndio kusaliwa kwa Sala. Ndio maana aya zikasema:

﴿فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ وَابْتَغُوا مِن فَضْلِ اللَّهِ وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

Fa-idha qudhiyati alssalatu faintashiroo fee al-ardhi waibtaghoo min fadhli Allahi waodhkuroo Allaha katheeran laAAallakum tuflihoona; *(Surat Al Jumuah 62:10)*

Tafsir: **Na Kisha Mtakapomaliza Kusali Basi Tawanyikeni kwenye Ardhi Na mtafute kutoka katika Fadhila za Allah Na Mumtaje Allah kwa Wingi Ili Mpate Kufuzu.**

Kisha *Allah Subhanah wa Ta'ala* analizungumzia Tukio lililotokea kwa kutuambia:

﴿ وَإِذَا رَأَوْا تِجَارَةً أَوْ لَهْوًا انفَضُّوا إِلَيْهَا وَتَرَكُوكَ قَائِمًا ۚ قُلْ مَا عِندَ اللَّهِ خَيْرٌ مِّنَ اللَّهْوِ وَمِنَ التِّجَارَةِ ۚ وَاللَّهُ خَيْرُ الرَّازِقِينَ﴾

Wa-idha raaw tijaratan aw lahwan infadhdhoo ilayha watarakooka qa-iman qul ma AAinda Allahi khayrun mina allahwi wamina alttijarati waAllahu khayru alrraziqeena. *(Surat Al Jumuah 62:11)*

Tafsir: **Na wanapoona Biashara Au Mambo ya Kipuuzi Wanatawanyika Kuyafuata Wakikuwacha Wewe peke yako Waambie Kua Kile kilichopo mbele ya Allah ni bora Kuliko Mambo ya Kipuuzi na Biashara Na Allah Ndie Mbora wa Kuruzuku.**

Nadhani tumefahamiana juu ya mtizamo huo wa Imam Al Ghazali wa Pili yaani Imam Fakhr Ad Din Al Razi ambae ni bigwa wa Kufafanua aya za Qur'an kwa kutumia Aya nyengine za Qur'an kama tulivyoona katika Mfano huu.

Kisha Imam Fakhr Ad Din Al Razi anendelea kutuambia kua: **'Ama kuhusiana na Manyoya ya Nguruwe basi mbali ya jua Wanazuoni Wanakubaliana kua ni Najis lakini hapo hapo Wanazuoni wametofautiana Juu ya kuyatumia kwani kulingana na Mtizamo wa Imam Abu Hanifa na Imam Muhammad Ash Shaybani basi wao wanasema kua Inakubalika.**

Lakini kwa upande wa Al Shafii basi kasema kua Haikubaliki kuyatumia. **Na Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa aitwae Abu Yusuf basi amesema kua:'Hakika mimi sipendi Kuyatumia lakini imesemwa nae Abu Hanifa kua inaruhusika.***''(Mafatih Al Ghayb)*

Na anasema Imam Al Faqih Al Aalamah Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii katika Al Hawi Al Kabir kua; '**Ni kama alivyosema Imam Al Muzani kua Nguruwe ni Najis zaidi Kuliko Mbwa Na amesema**

أَبِي هريرة أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: إِنَّ اللَّهَ حرم الخمر وثمنها، وحرَّم الميتة وثمنها، وحرم الخنزير وثمنه

Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameharamisha Mbwa na Bei yao, Ameharamisha Nguruwe na Bei Yao, na ameharamisha Ulevi na Bei Yake.

Na hii ni kwa sababu Kuweka Bei juu ya Nguruwe hua ni Ubaya zaidi kuliko kuweka juu ya Mbwa kwa sababu imekatazwa kunufaika nao katika baadhi ya hali ya mazingira fulani wakati imeruhusika kunufaika na Mbwa katika hali ya Maazingira Fulani. Ambapo Unajis wa Mbwa umethibitishwa kam tulivyoona hivyo Unajis wa Nguruwe ndio Unastahiki Zaidi.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Na mbali ya Hadith hio aliyoinukuu Imam Al Mawardi lakini pia kuna Hadith nyengine isemayo kua: 'Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua;

«إِنَّ اللَّهَ حرَّمَ الخمرَ وثمنَها ، وحرَّمَ الميتةَ وثمنَها ، وحرَّمَ الخنزيرَ وثمنَهُ»

Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameharamisha Ulevi na Bei yake, na pia ameharamisha Nyama ya Mnyama aliekufa na Bei yake na pia ameharamisha Nguruwe na Bei yake.'(*Sunnan Abu Daud)*

Ambapo kulingana na Maneno ya Hadith mbili hizi Tunaona kua Hukumu za Sharia ya *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya Maharamisho haya ni kuzuia Njia zote zitakazopelekea kuwapa urahisi Watu kufanikiwa kukifanya Kile kilichokatazwa. Na hivyo basi hapa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameweka wazi kua haikubaliki kunufaika na Vitu hivi vilivyoharamishwa si kwa kuvitumia tu bali pia kwa kuvitia bei na Kuviuza ili pesa zake zitumike na kunufaisha Mambo mengine. Hivyo hua haikubaliki kunufaika na kila Kitu kilichoharamishwa kwa njia moja ama nyengine.

Ambapo kuna Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا قُتَيْبَةُ بْنُ سَعِيدٍ، حَدَّثَنَا لَيْثٌ، عَنْ يَزِيدَ بْنِ أَبِي حَبِيبٍ، عَنْ عَطَاءِ بْنِ أَبِي، رَبَاحٍ عَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، أَنَّهُ سَمِعَ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَقُولُ عَامَ الْفَتْحِ وَهُوَ بِمَكَّةَ " إِنَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ حَرَّمَ بَيْعَ الْخَمْرِ وَالْمَيْتَةِ وَالْخِنْزِيرِ وَالأَصْنَامِ " . فَقِيلَ يَا رَسُولَ اللَّهِ أَرَأَيْتَ شُحُومَ الْمَيْتَةِ فَإِنَّهُ يُطْلَى بِهَا السُّفُنُ وَيُدْهَنُ بِهَا الْجُلُودُ وَيَسْتَصْبِحُ بِهَا النَّاسُ فَقَالَ " لاَ هُوَ حَرَامٌ " . ثُمَّ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم "عِنْدَ ذَلِكَ " قَاتَلَ اللَّهُ الْيَهُودَ إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ لَمَّا حَرَّمَ عَلَيْهِمْ شُحُومَهَا أَجْمَلُوهُ ثُمَّ بَاعُوهُ فَأَكَلُوا ثَمَنَهُ

Amesema Utaybah Ibn Said kua amesema Layth kua amesema Yazid Ibn Abi Habib kua amesema Ataa Ibn Abi Rabah kua amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: Nimemsikia Mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Mwaka wa *Fat-h ul Makkiya*, wakati akiwa katika Mji wa Makkah akisema kua: 'Allah na Mtume wake Wameharamisha Uuzwaji wa Pombe, Nyama ya Wanyama waliokufa, Nguruwe na Masanamu.

Hivyo kuna mtu akasema: *Ya Rasul Allah!* Hivi Jee unasemaje kuhusiana Na Mafuta ya Mnyama aliekufa?, kwani sisi hua tunatumia kwa ajili ya Kupaka Majahazi yetu yasiingie Maji, Yanatumika Kulainishia Ngozi za Wanyama na pia Watu wanatumia Kuwashia Taa.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: La! Yameharamishwa!**

Kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema katika wakati huo: 'Namuomba Allah awapige vita Mayahudi, kwani Allah amewaharamishia Mafuta hayo, lakini wao wakayayeyusha na kisha wakayauza Na wakala Pesa zilizotokana na Mauzo yake''*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo amesema Shaykh ul Islami Imam Abu Zakariyah Yahya Ibn Sharafa An Nawawi kuhisiana na Hadith hii kua: '**Waislamu wanakubaliana juu ya Uuzwaji wa Maiti ya Mnyama, Pombe na Nguruwe kua ni Haramu'**

'Na Wanazuoni wanasema kua Jumuisho la kuharamishwa kuuzwa kwa Wanyama Waliokufa hua linajumuisha hata kuiuzza miili ya Makafiri kama tutamuua na kisha Makafiri wenzake

wakata Mwili wake kwa kuuliipia au kwa fidia kwani imetajwa katika Hadith kua Nawfal Ibn Abd Allah aliuliwa na Waislam katika Vita vya Khandak na Makafiri wakataka kuoa Dirham Elfu kumi kwa ajili ya Mwili wake lakini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* akakataa kuzipokea, na hivyo akawapaMwili huo bure bila ya Malipo.'*(Sharh Sahih Muslim)*

Na amesema pia Al Qadhi Iyad kua: **'Hadith hii inathibitisha kua kila kile kisochoruhusika kuliwa au kunufaika nacho hua hakiruhusiki kuuzwa , na wala hairuhusii kutumia Malipo yake kama vile ilivyotajwa katika hadith.'**

Lakini kwa upande wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafi basi yeye amesema kua: **'Maana ya Hadith hii inaelekea kutilia mkazo kile kilichotafsiriwa na wengi miongoni mwa Wanazuoni kutokana na maneno yasemayo kua 'Imekatazwa' ambayo yanahusiana na Kuuza na si kuhusiana na Kunufaika navyo.'***(Fat-h Al Barr)*

Na Imam Abu Daud ameripoti Hadith hii kupitia kwa Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* huku ikimalizia na maneno yasemayo kua:

نهى رسول الله –صلى الله عليه وسلم– عن خمْسٍ: عن ثَمَنِ الكلبِ، وثَمَنِ الخنزيرِ، وثَمَنِ الخمرِ، وعن مَهْرِ البَغِيِّ، وعن عَسْبِ الفَحْلِ

'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua Allah anapoharamisha Kukila Kitu basi huharamisha na Bei yake pia. **Na Imam Ibn Shaybah pia amenukuu ikiwa na maneno yamaliziayo kwa kusema kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua *Allah Subhanah wa Ta'ala* anapaharamisha Kitu huharamisha Na bei yake pia.'***(Jamii Al Ulumu wa Al Hukm)*

Hivyo amesema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Bakr Al Ansari Al Qurtubi Al Maliki kua: '**Kuna Makubaliano ya Wanazuoni kuhusiana na Kuharamishwa kwa Mafuta ya Nguruwe, na katika Kulithibitisha hili basi Imam Malik na Wanafunzi wake wamesema kua Kama ikiwa Mtu ataapa hatokula Mafuta ya Nguruwe na kisha akala Nyama ya Nguruwe basi kiapo chake hua Hakivunjiki kwa Kula Nyama hio, lakini kama akiapa kua hatokula Nyama ya Nguruwe na kisha akala Mafuta yake basi Kiapo chake huvunjika na hii ni kwa sababu Nyama yenye Mafuta Mafuta hua bado inaitwa Nyama, kwani Mafuta hua ni sehemu ya Maumbile ya Nyama lakini hua si vyenginevyo, na Allah ameharamisha Nyama ya Nguruwe.'***(Jamii Al Ahkami)*

Na amesema Imama Abu Qasim Sulayman Ibn Ahmad Ibn Ayub Ibn Mutayyir Al Lakhmi Ash Shami At Tabrani Al Shafii kua Amesema Abd Allah Ubn Amr *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amesema kua: '*Allah Subhanah wa Ta'ala* ameharamisha Bei za Vitu Vitano: Bei ya Mbwa; Bei ya Nguruwe; Bei ya Vilevi; Bei ya Kahaba na Bei ya Manii ya Farasi Dume Asiekua Mzee.'*(Al Awsat, na Sahih Jamii)*

Na amesema Imam Ali Ibn Ahmad Ibn Hazim Al Andalus kua: '**Wanazuoni Wanakubaliana kua Nyama, Mafuta, Mifupa Migumu na milaini, Tezi Laini na Ubongo wa Mnyama aliekufa kua ni Haram. Na pia Nyama, Mafuta, Mifupa laini na Migumu, Tezi, Ubongo na Mishipa ya Nguruwe kua Vyote ni Haram, na ni Najis'***(Maratib Al Ijmaa)*

Imam Ibn Hazim anaendelea kutuambia kua: **'Hivyo hairuhusiki kutumia sehemu yeyote ya Nguruwe, iwe kichwa, Miguu, Maziwa yake na hata Manyoya yake, iwe Nguruwe huyo ni Dume**

au Jike, Mdogo au Mkubwa, na wala hairuhusiki kutumia Manyoya yake hata katika Kushonea Viatu au kwa kufanyia chochote kile'*(Maratib Al Ijma)*

Ambapo imesemwa katika *Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyyah* kua: '**Manyoya ya Nguruwe ni Najis hivyo hairuhusiki kuyatumia kwa sababu Kuyatumia kwake hua ni sawa na kuitumia Najis yenyewe.**

Ambapo Kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wao wanasema kua Kama Soksi ya Ngozi ikishonwa kwa Uzi uliotokana na Manyoya ya Nguruwe, basi Sehemu husika hua haiwezekani Kutoharishwa kwa Maji wala kwa Mchanga.

Lakini hata hivyo itaruhusika Kusali Soksi Katika Sala za Sunna tu, kwani inawezekana Kusamehewa hali hio.

Ama kwa upande wa Madhhab ya Imam Hanbal basi ni kua kama ikiwa Soksi hio iliposhonwa ilikua Imaji basi itabidi ikoshwe na inaruhusika Kutumia Kitu cha Kusugulia kama Ilippshonwa ilikua imeshakauka.

Kwa sababu inapokua kavu basi Najis hua haisambai,lakini haitoruhusika kutumia kama itakua imaji kwa sababu Najis husambaa kwa Maji Kwa Upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao Wanaruhusu kutumia Manyoya ya Nguruwe kwa Dharurah.

Ambapo kwa upande wa Wafuasi wa Imam Malik basi wao Wanasema kua Manyoya ya Nguruwe ni Tohara.

Hivyo kama yakikatwa kwa Mkasi basi inaruhusika kutumika hata kama ikiwa Nguruwe huyo ameshakufa, kwa sababu Manyoya hua hayanautofauti kwa Mnyama aliekufa au alie hai Lakini hua inapendekezwa kuyakosha kwa sababu ya kutoa wasiwasi kua kama ni Tohara Ama la, lakini kama Manyoya hayo yatakua yamenyonyolewa basi bila ya Shaka yatakua si Tohara.

Hivyo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik tu ndio wanaosema kua Manyoya ya Nguruwe ni Tohara pale Nguruwe huyo atakapokua yuhai, na kama Manyoya hayo yamekatwa na wala hayaja nyonyolewa, kwani yakinyonyolewa basi mizizi yake husababisha kutokua Tohara.' *(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyyah)*

Na kwa upande mwengine basi kuna Hadith Sahih isemayo kua:

حَدَّثَنَا إِسْمَاعِيلُ بْنُ مُوسَى السُّدِّيُّ، حَدَّثَنَا سَيْفُ بْنُ هَارُونَ، عَنْ سُلَيْمَانَ التَّيْمِيِّ، عَنْ أَبِي عُثْمَانَ النَّهْدِيِّ، عَنْ سَلْمَانَ الْفَارِسِيِّ، قَالَ سُئِلَ رَسُولُ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ عَنِ السَّمْنِ وَالْجُبْنِ وَالْفِرَاءِ قَالَ " الْحَلاَلُ مَا أَحَلَّ اللَّهُ فِي كِتَابِهِ وَالْحَرَامُ مَا حَرَّمَ اللَّهُ فِي كِتَابِهِ وَمَا سَكَتَ عَنْهُ فَهُوَ مِمَّا عَفَا عَنْهُ

Amesema Ismail Ibn Musa Al Sudiyu kua amesema Seif Ibn Harun kua amesema Sulayman At Taymi, Kua amesema Abi Uthman An Nahdi kua: 'Amesema Salman Al Farsy *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliuliziwa kuhusiana na Samli, Jibini na Punda Mwitu.'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akajibua kwa kusema kua: 'Halali ni kile alichokihalalisha Allah katika Kitabu Chake, na Haram ni kile alichokiharamisha Allah katika Kitabu chake, na kila kile ambacho hakijazungumziwa basi hua kimesamehewa.'*(Sunan Ibn Majah, Imam At Tirmidhii, Imam Al Bayhaqi, Imam Abd Razzaq na Imam Al Hakim)***

Na anasema Mujaddid Ad Din Mujtahid Imam Abu Bakar Ibn Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Al Mundhiri Al Nishapuri Al Shafii kua: '**Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na Kuharamishwa kwa Nguruwe kwani Nguruwe ameharamishwa kwenye Qur'an, Kwenye Sunnah na kwenye Ijmaa (Makubaliano ya Waislam).**

Ila wametofautiana kuhusiana na Manyoya yake, kwani kuna Kundi ambalo linaruhusu Kutumika Manyoya hayo katika Kushonea, na miongoni mwao ni Imam Hasan Al Basr, Imam Malik, Imam Al Awzai na Nuuman Ibn Thabit Abu Hanifa, wao hawa wameruhusu. Nasi tumenukuu kutoka kwa Imam Al Asha'bi ambae aliulizwa kuhusiana na Kibuyu cha Ngozi ya Nguruwe kitokanacho Nchini Azabaijan ambacho hutumika Kubebea Mafuta. Ambapo nae akasema: 'Hamna Tatizo juu yake.'

Na pia

وروى حسن ، قول ابن عباس: ''انما حرم ما يؤكل منها وهو اللحم، فاما الجلد والقد والسن والعظم والشعر والصوف فهو حلال''، مشيرا الى ان العلماء اجمعوا على انه يجوز الخرز بشعر الخنزير، حسب رأيه.

Amesema Hasan Al Basr kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: "Kilichoharamishwa ni Nyama tu, lakini ama Ngozi, Jino, Mfupa, Nywele na Sufi, ni halali." Hivyo Imam Hasan Al Basr amesema kuwa Wanazuoni wamekubaliana kwa kauli moja kwamba inajuzu kutengeneza shanga kwa nywele za Nguruwe, kwa maoni yake.

Ama kwa upande wa Imam Al Awzai yeye ameruhusu kukinunua kinapouzwa Lakini hapendelei Kuuzwa kwake.

Na kwa Upande wa Nuuman basi yeye hapendelei kuuzwa kwake wala kununuliwa kwake.

Ambapo kwa upande wa Imam Muhammad Ibn Sirin, Imam Al Hakam, Imam Ahmad, Imam Is-haq Ibn Rahawayh basi wao hawapendelei juu ya Matumizi ya Manyoya ya Nguruwe Kwani wanasema kua Tunapendelea kua vitu vishonwe kwa Kutumi Nyuzi za Makuti ya Mitende.

Abu Bakr yeye amesema kua: Hairuhusiki Kutumia Kitu kilichoharamishwa kwa njia yeyote Ile, na hii ni kulingana na Hadith ya Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* ambayo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliulizwa kuhusiana na Mafuta ya Nguruwe ambayo watu hutumia kupaka Majahazi yao, Kulainisha Ngozi na kwa ajili ya Manufaa mengine, na *Rasul Allah Salallahu Aalayhi wa Salam* akasema Kua La! Hairuhusiki.

Na kisha akataja maneno ya Hadith aliyoyasema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* juu ya Mayahudi ambayo yanathibitisha wazi kua hairuhusiki kuyatumia, wala Kuyauza wala kuyanunua.

Na Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* inathibitisha hivyo kwa kusema kua: ‘Amesema Yahya Ibn Muhammad kua amesema Musaddad kua amesema Bishr Ibn Mufaddal kua ametuambia sisi ku Khalid Al Hadha amesema kua, amesema Barakah kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua:

رأيت رسول الله صلى الله عليه وسلم جالسا عند الركن، فرفع بصره إلى السماء فضحك، فقال: "لعن الله اليهود – ثلاثا – إن الله حرم عليهم الشحوم فباعوها وأكلوا أثمانها، وإن الله إذا حرم على قوم شيئا حرم عليهم ثمنه

Nilimuona *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekaa katika pembe ya Al Kaaba karibu na Hajar Al Aswad. Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Akanyanyua Macho yake Juu kuelekea Mbinguni na akacheka na kusema: Allah awalaani Mayahudi, Allah Awalaani Mayahudi, Allah Awalaani Mayahudi, kwani Allah aliwaharamishia Mafuta ya Nguruwe, lakini wao wakayauza‹na Wakala Malipo waliyolipwa kwa kuuza Mafuta hayo Na wakati Allah anapoharamisha Kitu kwa Waja wake basi huwaharamishia pia na bei ya kitu hicho.’(Sahih Bukhari na Muslim, Sunna Imam Abu Daud) *(Al Wasit Fii Sunnan,wa Al Ijmaa, wa Al Ikhtilafi - Imam Ibn Al Mundhiri)*

Ambapo wanasema Imam Abdul Hamid Al Makki Al Sharwani Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Qasim Al Abbadi Al Shafii kua: ‘**Ama kuhusiana na katazo la Kutumika Kitu kilichoharamishwa kama kitokanacho na Ngozi au Nwele za Mbwa Au Nguruwe Bila ya kutokana na Dharurah yeyote, basi hua ni Katazo la matumizi ya kitu kama Shitayh (Brashi) ambacho hutengenezwa kutokana na Manyoya ya Nguruwe.**

Lakini kama ikiwa hakuna Nyuzi za Plastiki au nyenginezo za Kutengenezea kitu hicho, basi hii hua ni dharurah inayoruhusu Kutumika kwa Nywele za Nguruwe, na kugusana nayo, na hivyo Mtu atasameheka kama akiigusa hata kama ikiingia Maji.’ *(Hawashi Al Sharwani Wa Al Abbadi aAla Tuhfah Muhtaj Bi Sharh Minhaj)*

Na anasema *Maliki Al Ulamaa* Imam Alaa Ad Din Abu Bakr Ibn Masud Al Kasani al Hanafi kua: ‘**Ama kuhusiana na Nguruwe basi imenukuliwa kutoka kwa Imam Abu Hanifa kua Nguruwe ni Mnyama mwenye sifa ya kua ni Najis ya Kimaumbile, kwa sababu *Allah Subhanah wa Ta'ala* kamuelezea kua ni Najis, na hivyo hua hairuhusiki kutumia Manyoya na kila kitu chake Lakini hata hivyo, Imam Abu Hanifa ameruhusu kutumika kaa Manyoya ya Nguruwe na Washonaji kutokana na Dharurah.**

Na pia imenukuliwa kutoka kwa Imam Abu Yusuf (Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa) kutoka katika chanzo tofauti kua yeye hapendi matumizi ya vitu vinavyotokana na Nguruwe na hairuhusiki kuuza kitu chochote kutokana nae Nguruwe na hii ni katika Nukuu zake zote.

Na imenukuliwa kutoka kwa Wanazuoni wetu (Wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa) kua Sehemu za Manyoya ya Nguruwe ni Tohara kwa sababu ya kua Manyoya hua hayana Damu, lakini hata hivyo Mtizamo sahih ni kua Manyoya ya Nguruwe si Tohara kutokana na Damu au na umajimaji bali ni Kutokana na Maumbile yake.’*(Badai Al Sanai)*

Na amesema Muwaffaqa Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: **‘Manyoya ya Kila Mnyama hua ni sawa na Kila kitu chake, hivyo Mnyama kama akiwa Tohara basi na Manyoya**

yatakua Tohara. Na Mnyama akiwa ni Najis basi Na Manyoya yatakua ni Najis, na hakuna tofauti baina yake juu ya kua kama Mnyama yuko hai ama la.' ***(Al Mughni)***

Hivyo tumeona Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii hapo kabla, na Mtizamo wa Madhhab ya Ahu Hanifa na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kupitia kwa Imam Ibn Qudamah. Lakini tunapoangalia Mtizamo huo wa Imam Ibn Qudamah basi tunaona unapishana na Mtizamo wa Imam Burhan Ad Din Ibn Muflih Al Hanbal ambae ni Mwanazuoni Mahiri wa Madhhab Ya Imam Ibn Hanbal pia, kwani yeye anasema kua: '**Aqida yetu ni kua Mbwa na Nguruwe na kila kinachotokana nao hua ni Najis, ambapo kuhusiana na Manyoya yao basi ndio yaliyochaguliwa kua Tohara na Abu Bakr na Shaykh wetu.'***(Al Furuu)*

Na tunapomuangalia Mwanazuoni mwengine wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal ambae ni Imam Sulayman Al Mardawi Al Hanbali basi tunaona kua yeye anasema kua: **'Mtizamo sahih wa Madhhab yetu kuhusiana na Mbwa na Nguruwe basi Wote ni Najis na kila kitokanacho na wao hua ni Najis, na huu ndio Mtizamo wa Wengi miongoni mwa Masahaba Radhi Allahu Anhum na wote wana uhakika juu ya hilo.'***(Al Insaf)*

Ama tunaporudi katika Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Abd Allah Al Kharashi Al Maliki kua: '**Sufi, Manyoya, Nywele hata kutoka kwa Nguruwe hua ni Halali, kama ukiyakata na hivyo kutoka kwa Wanyama wote hua ni halali, na hata kama ukiyakata baada ya kufariki kwa Mnyama husika, kwa sababu vitu hivyo hua haviwezekani kua na Uhai, na vitu visivyokua na Uhai hata baada ya kufa kwa Mnyama hua haviwi haram pale Mnyama atakapokua hai na wala pale atakapofariki.**

Na kutokana na kua vitu hivyo hua halali kabla ya kufariki kwa Mnyama husika basi hua halali baada ya kufariki kwake pia kulingana na kanuni ya Mtizamo wa Muendelezo wa Vitu.

Hivyo hakuna utofauti katika Madhhab yetu juu ya Manyoya, Sufi au Nywele, lakini Utohara wake hua ni kwa sharti la kua Manyoya hayo iwe Lazima Yamekatwa bila kua na mzizi wake, hata kama baada ya kunyonyolewa' (*Khashiya Al Kharashi aAla Mukhtasar Al Khalil)*

Ama kwa upande wa Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qalyubi Al Masri Al Shafii kua: '**Manyoya ya Nguruwe hua ni Najis, ambapo Unajisi huo huweza kuhamishika katika vitu vyengine pale unapoingia Maji.'(***Imam Al Shatiri katika Al Yaqut Al Nafis).

Hivyo kama ikiwa Brashi zenye kutokana na Manyoya ya Nguruwe zitatumika katika kupakia Mafuta Nyama, Vyakula Vyenginevyo basi, Nyama hio na vyakula hivyo vyenginevyo vilivyopakwa kwa Kutumia Brashi hio hua ni Najis na Haram Kuliwa.'*(Hashiyah Al Qalyubi, Hashiyah Al Sharh Al Mahali)*

Kwani Huo ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Manyoya ya Nguruwe, ambapo Wanazuoni wa Imam Al Shafii wamekua na utofauti kimtizamo juu ya Unajisi wa Nguruwe na kila kitu chake, ambapo Mtizamo wao ni Mmoja tu ambao ni kua Nguruwe na kila kitu chake ni Najis, Mtizamo ambao ni tofauti na Mtizamo wa Madhhab mengineyo, hivyo unapofuatilia zaidi katika Vitabu vya Fiqh vya Madhhab ya Imam Al Shafii basi unaona kua haikuzungumziwa sana kuhusiana na Nguruwe, jambo ambalo ni tofauti na namna ilivyozungumziwa na Vitabu vya Madhhab mengine.

Na hii ni kutokana na kua Madhhab mengine wao wamekua na Mitizamo tofauti yaa ya Nguruwe mwenyewe, Nyama yake, Manyoya yake n.k Kwa mfano katika Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal kuhusiana na Manyoya ya Nguruwe tumeona kua wao Wana mitizamo miwili tofauti, ambapo wa

kwanza ni kama Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik yaani kua Manyoya ya Nguruwe ni Tohara pale itakapokua Manyoya hayo hayakashikamana na Mizizi yake.

Mtizamo Wa pili ni kama Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii yaani kua Si Tohara bali ni Najis, iwe yameshikamana na mizizi ama la.Hivyo mbali ya kua Brashi ziko aina nyingi sana kwani ziko za Kupakia Rangi, Kusugulia Meno, Kupakia Mafuta Vyakula kama Nyama, Samaki, Mikate n.k kuna za Kusafishia Vitu tofauti, Kuna za Kuchania Nywele n.k.

Lakini pia Brashi zinatofautiana na asili yake kwani kuna Brashi zitokanazo na Nyuzi za Miti, Kuna Brashi zitokanazo na Nylon yaani Plastic, Brashi za Chuma na pia kuna Brush zitokanazo na Manyoya na Nywele za Wanyama ikiwemo Manyoya ya Nguruwe. Hivyo Waislam inabidi kua na umakini juu ya jambo hili kwani kila kilichoharamishwa basi hua pia ni Haramu Kukiuza, na kutumia pesa ulizokiuzia na ni haram kukinunua na kukitumia.

Naam amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* kua:

﴿هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ لَكُمْ مَّا فِى ٱلأَرْضِ جَمِيعاً ثُمَّ ٱسْتَوَىٰ إِلَى ٱلسَّمَآءِ فَسَوَّاهُنَّ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ﴾

Huwa Alladhii Khalaqa Lakum Ma Fi Al Ardhi *(Surat Al Baqara 2:29)*

Tafsir: ***Yeye (Allah Subhanah wa Ta'aala ndie Aliekumba kwa ajili yenu vyote vilivyopo juu ya Ardh****i*

Haya ni maneno ya Qur'an ambayo ndio yaliyotoa Kanuni ya Fiqh isemayo kua: Kila kitu ni Halali hadi pale itakapokua kua Uthubitisho wa Hakika juu yake Na Kanuni hii ndio inayotupelekea katika kuangalia kuhusiana na Mafuta ya Mnyama alieharamishwa ambae ni Nguruwe ambayo mengi hua ni yenye kutoka katika Sehemu ya Ndani ya Ngozi ya Nguruwe, na Wanazuoni wanakubaliana kua Mafuta haya hua ni Najis na ni Haramu.

Na bila ya shaka Mafuta ya Nguruwe ni Mafuta ambayo hua yanatumika katika bidhaa kadhaa tunazotumia Ibn Adam, kwa mfano

Sabuni za Kukogea na kunyolea, Mafuta ya Kulainisha na Kung'arisha Ngozi Dawa za Misuaki, Vyakula vya aina tofauti kama Vilivyohifadhiwa kwenye Vibati, Matunda yaliyohifadhiwa kwenye Vibati, Biskuti, Chocolate, Peremende, Ubani, na hata Multi Vitamins n.k.

Na kwa kua Bidhaa hizi hua pia zinatumiwa na Waislam na Waislam ni Haram kwao kula na kutumia Kitu kitokanacho na Nguruwe, na Wazalishaji Bidhaa wa Nchi za Magharibi kutakiwa lazima kuainisha Viambatanisho walivyotumia kwenye bidhaa zao,basi iliwabidi Wenye Viwanda.

Kunbadilisha Mfumo wa Kutoandika Neno Nguruwe kwenye Bidhaa zao, kwani watakosa soko katika Nchi za Kiislam, basi wakaamua kuandaa Kodi Namba maalum zenye kuainisha kwa Siri aina ya Viambatanishi vya Nguruwe ndani ya Bidhaa husika bila kutaja kua kinatokana na Nguruwe.

Hivyo kabla ya kuendelea juu ya Mitizamo ya Wanazuoni kuhusiana na Mafuta ya Nguruwe basi na Tubainishiane Kodi namba hizo ili tuzijue kabla ili tupate kuepuka Utumiaji wa Vuambatanishi Vitokanavyo na Nguruwe ambavyo hua na aina 52 za E (European Ingredient Codes) Kodi zifuatazo:

E100, E110, E120, E140, E141, E153
E220, E213, E214, E216, E234, E252, E270, E280
E325, E327, E334, E335, E336, E337
E442, E430, E431, E432, E433, E434, E435, E436, E440, E470, E471, E472, E473, E474, E475, E476, E477, E478
E481, E482, E483,
E491, E492, E493, E494, E495
E542, E570, E572
E631, E635
E904.

Naam..hizi ni Codes ambazo kwa wale wanaoishi Ulaya hua wanazijua hivyo na mimi na wewe tunaoishi Afrika na kununua Vitu kutokana na Uzuri wa Mapambo ya Rangi tofauti ya Mifuko yake na kwenye Vibati vyake basi inatubidi kujua pia kwa sababu vyenginevyo tutakua tunanunua vile tulivyoharamishiwa kununua,kula na kutumia, na hivyo kujiharamishia na kujichafulia kila kitu chetu tangu miili hadi Ibada pia.

Kwani amesema Imam Bukhari na Muslim kua:

حَدَّثَنَا أَبُو نُعَيْمٍ، حَدَّثَنَا زَكَرِيَّاءُ، عَنْ عَامِرٍ، قَالَ سَمِعْتُ النُّعْمَانَ بْنَ بَشِيرٍ، يَقُولُ سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ " الْحَلاَلُ بَيِّنٌ وَالْحَرَامُ بَيِّنٌ، وَبَيْنَهُمَا مُشَبَّهَاتٌ لاَ يَعْلَمُهَا كَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ، صلى الله عليه وسلم يَقُولُ فَمَنِ اتَّقَى الْمُشَبَّهَاتِ اسْتَبْرَأَ لِدِينِهِ وَعِرْضِهِ، وَمَنْ وَقَعَ فِي الشُّبُهَاتِ كَرَاعٍ يَرْعَى حَوْلَ الْحِمَى، يُوشِكُ أَنْ يُوَاقِعَهُ. أَلاَ وَإِنَّ لِكُلِّ مَلِكٍ حِمًى، أَلاَ إِنَّ حِمَى اللَّهِ فِي أَرْضِهِ مَحَارِمُهُ، أَلاَ وَإِنَّ فِي الْجَسَدِ مُضْغَةً إِذَا صَلَحَتْ صَلَحَ الْجَسَدُ كُلُّهُ، وَإِذَا فَسَدَتْ فَسَدَ الْجَسَدُ كُلُّهُ. أَلاَ وَهِيَ الْقَلْبُ "

Amesema Abu Nuaymi kua amesema Zakarriyah kua amesema Aamiri kua amesema Nuuman Ibn Bishr *Radhi Allau Anhu* kua nimemsikia mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: **Vya Halali viko wazi na Vya Haramu viko wazi, na baina yake vitu hivyo kuna visivyokua wazi na hivyo kua na ni vyenye shaka kaa kutojulikana na watu wengi.**

Hivyo yule atakaeachana na yale yenye shaka basi atakua salama na Dini yake na Heshima yake, na yule atakaetumbukia ndani ya yaliyokatazwa basi atakua kama Mchunga ambae anachunga Wanyama wake karibu ya Mipaka na atajikuta ameshavuka mipaka bila kujijua.

Kwa hakika Kila Mfalme hua na mipaka ya Himaya yake na Mipaka ya Himaya ya Allah katika Ardhi yake ni Makatazo yake. **Na kwa hakika katika Mwili kuna kipande cha Nyama ambacho kama kitakua Safi basi Mwili mzima utakua safi, lakini kama kiki chafuka basi Mwili mzima huchafuka, Kwa hakika Kipande hicho ni Moyo.'***(Sahih Bukhari na Muslim)*

Ambapo amesema pia Imam Ibn Naqib Al Masri Al Shafii kua: '**Kila kitu hua iinahesabiwa ka na Asili ya Utohara hadi pale utakapothibitika Unajis wake**.' *(Umdat Salik wa Uddat An Nasik)*

Hivyo katika Kuangalia hali ya Unajis wa Mafuta ya Nguruwe ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua Nguruwe na kila kitu chake hua ni Najis. Na tunaezunguzia kuhusiana na Vitu tofauti tunavyotumia kwa aidha Kula au Kujipaka ambapo kwa baadhi hua Na Viambatanishi vyenye Mafuta ya Nguruwe, lakini wengi wetu ai wenye kujua juu yake kwani baadhi ya vitu hivyo hua vinatumia Viambatamishi vya Mafuta ya Mimea pia na pia kutokana na baadhi ya Mafuta ya Wanyama wasiokua Haram.

Kwa maana hio basi kwa Mfano kama Kitu kitakua Kina viambatanishi vya Mafuta kwa Mfano Sabuni, Shampoo, Vipodozi Vyakula n.k.

Lakini Ikawa hakuna Uhakika wa Kua kama Mafuta hayo ni ya Mimea au Mnyama aliekua Halali kuliwa na Amechinjwa kihalali, basi Kitu husika kitahesabika kua ni Halali Kuliwa na Kutumika.

Lakini kama ikiwa hakuna uhakika wa kua kama Mafuta hayo yametokana na Nguruwe au Kama si Nguruwe lakini Mnyama hakuchinjwa Kiislam ama la, basi Hukumu ya Kitu hicho itakua ni Najis na Haramu kuliwa na Kutumika pia.

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Yahya Muhammad Ibn Zakarriyah Zayn Ad Din Al Sunayki Al Ansari Al Shafii kua: '**Hairuhusiki Kwa Muislam Kujipaka Najis kwenye Mwili wake au kwenye Mavazi yake**.*'(Ianat Al Talibin)*

Na bila ya shaka tumeshafafanua kuhusiana na Kula kitu ambacho Ni Najis ikiwemo Nguruwe, Mnyama ambae hakuchinjwa kwa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala,* Au aliekufa n.k kua ni Haram. Na juu ya hili kuna Makubaliano ya wanazuoni kama alivyosema Mujaddidd Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi Al Shafii na kama ilivyosemwa katika *Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaitiyah*.

Kwa maana hio basi hii inamaanisha kua Kama Mtu Ukifulia, Ukikogea Sabuni Ukikogea Shampuu, Ukijipaka Mafuta, au Vipodozi vyenye Viambatanishi vya Mafuta ya Nguruwe au Mnyama ambae hajachinjwa Kislam, basi hutokua Tohara na Ibada zako ni Batili kwa sababu ya kua Umejipaka Najis.

Na hapa Sasa Waislam ndio tunaona umuhimu wa Kua Makini sana katika Kuishi kwetu ndani ya Maisha haya yaliyojaa mchanganyiko wa Vitu tunavyotumia kutokana na mazoea. Hivyo tusiishi kwa Mazoea kua unakogea Shampuu yeyote, Unafulia na kukogea Sabuni yeyote unajipodoa kwa Kipodozi chochote n.k bila kuchunguza kitu asili yake. Kwani kama tukiishi hivyo basi tutajikuta kua tumejifilisi Kiamali hapa Duniani na Kuangamia Kesho Akhera.

Kwani tumezungumzia zaidi kuhusiana vitu vya Kujipaka na kukogea kwa sababu Kuhusiana na Chakula cha Haram basi anasema Hujjat Ul Islami Imam Abu Hamid Muhammad Al Ghazali Al Shafii kua: '**Kama Ikiwa Mtu atakunywa Mvinyo na kisha akatia Udhu, na Kusali basi Sala yake itahesabika kwa sababu kile kilichokua Tumboni hakina Hukumu juu yake.'** (*Al Wasit Fii Madhhab Al Shafii)*

Ila sasa kukubalika kwa Sala ya Mtu huyo ama la basi ni juu ya *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

MUBTILAT SALAT – NAJIS YA NGURUWE NA AL ISTIHALAH

❖❖❖❖

Amesema *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika kitabu chake kitukufu kua:

﴿وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۖ نُّسْقِيكُم مِّمَّا فِي بُطُونِهِ مِن بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ لَّبَنًا خَالِصًا سَائِغًا لِّلشَّارِبِينَ﴾

Wa-inna lakum fee al-anAAami laAAibratan nusqeekum mimma fee butoonihi min bayni farthin wadamin labanan khalisan sa-ighan lilshsharibeena *(Surat An Nahl 16:66)*

Tafsir; **Na Kwa Hakika Kuna Kwa ajili yenu katika Ngombe Mafunzo Tunakupeni Kinywaji Kilichomo Matumboni mwao Kutokana na baina ya Kinyesi Na Damu Maziwa Safi kabisa Matamu kwa Wanaokunywa.**

Naam..tunaiangalia aya hii, ambayo kwa baadhi wanaweza kujiuliza jee imehusiana na nini na Mafuta ya Nguruwe? Hivyo jibu la suali hili ni kua tumeanza na Aya hii kwa sababu Aya hii inabeba moja kati ya Hukumu Muhimu sana ya Fiqh iitwayo *Al Istihalah.*

Al Istihalah maana yake hua ni Badiliko la Kitu kutoka katika hali ya Asili yake ya kimaumbile kua Najis na Haram na Kubadilika na kuingia katika hali ya kua ni Kitu chengine Kimaumbile, Kijina na Kimuonekano na hivyo kua ni Halali.

Na ndio maana akasema Mujaddid Ad Din Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kuhusiana na Aya hii ya 66 ya Surat An Nahl kua: '**Maziwa ni Mchanganyiko wa Kinyesi na Damu vitu ambavyo vimeingia katika Hali ya stihal (Mabadiliko) na kuyatoa Maziwa nje Mnyama yaliyo katika hai ya Usafi.'***(Fath Barr)*

Na akasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: **'Wanazuoni wanakubaliana kua Istihalah hutokea katika uzalishwaji wa Maziwa ndani ya Matumbo ya Wanyama. Na hivyo Ijapokua Kinyesi na Damu zinapotoka Nje ya Miili ya Wanyama hua ni Najis, lakini kile kinachotoka baada ya kutokea hali ya Istihalah kutoka katika Kinyesi na Damu huingia katika hali ya kua ni Maziwa ambayo ni halali kama yakizalishwa na Myama halali.'**(Al Majmuu)

Na bila ya shaka tunapoangalia Hadith basi tunaona anasema Imam Ibn Majah kua

حَدَّثَنَا الْعَبَّاسُ بْنُ عُثْمَانَ الدِّمَشْقِيُّ، حَدَّثَنَا الْوَلِيدُ بْنُ مُسْلِمٍ، حَدَّثَنَا عَنْبَسَةُ بْنُ عَبْدِ الرَّحْمَنِ، عَنْ مُحَمَّدِ بْنِ زَاذَانَ، أَنَّهُ حَدَّثَهُ قَالَ حَدَّثَتْنِي أُمُّ سَعْدٍ، قَالَتْ دَخَلَ رَسُولُ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ عَلَى عَائِشَةَ وَأَنَا عِنْدَهَا فَقَالَ " هَلْ مِنْ غَدَاءٍ " . قَالَتْ عِنْدَنَا خُبْزٌ وَتَمْرٌ وَخَلٌّ . فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ـ صلى الله عليه وسلم ـ " نِعْمَ الإِدَامُ الْخَلُّ اللَّهُمَّ بَارِكْ فِي الْخَلِّ فَإِنَّهُ كَانَ إِدَامَ الأَنْبِيَاءِ قَبْلِي وَلَمْ يَفْتَقِرْ بَيْتٌ فِيهِ خَلٌّ "

Amesema Abbas Ibn Uthman Ad Dimashq kua amesema Al Wahid Ibn Muslim kua amesema Anbasa Ibn Abd Rahman kua amesema Muhammad Jbn Zadan kua amesema Ummu Saad *Radhi*

Allahu Anha **kua: 'Nilienda mimi kwa Aisha na nilipokutana nae nikamuuliza: Jee una chakula chochote?'**

Ambapo nae akasema: 'Naam..Tuna Mkate na Tende na Siki.'

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: 'Siki ni kitoweo Kilichobarikiwa! Ya Allah ibariki Siki, kwa sababu Siki ndio Kitoweo cha Mitume waliotangulia kabla yangu, na hakuna Nyumba itakayo kua na Umasikini kama ikiwa na Siki ndani yake.**'*(Sunnan Ibn Majah)*

Ambapo ndani yake hadith hii tunaona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* anaisifu n kuiombea Dua Siki. Na Siki inayozungumziwa hapa hua ni yenye Kutokana na Juisi ya Tende ambayo baada ya kukaa kwa mda mrefu hugeuka hali yake na kua Pombe. Na ikiendelea kukaa zaidi hua ndio inageuka Siki.

Hivyo hapa Juisi ya Tende ambayo halali iliyobadilika hali (Istihalah) kua Pombe ambayo ni haramu imefanya istihalah tena na kua Siki ambayo ni Halali.

Na ndio maana akasema Imam Al Bayhaqi kua: '**Amesema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: Asinywe Mtu yeyote Siki iliyotokana na Pombe hadi pale Allah Subhanah wa Ta'ala atakapoibadilisha Pombe hio katika kua ni Siki Yaani hadi Pombe hio iwe Siki kweli kweli, na hapo ndio Siki itakapokua Halali. Hivyo Muislam hua hana kosa pale atakaponunua Siki kutoka kwa Ahl Al Kitab pale itakapokua ana uhakika kua Ahl Al Kitabu hao wamesuburi hadi Pombe hio imegeuka na kua Siki.'***(Imam Al Bayhaqi)*

Na pia mfano mwengine wa Istihalah katika Hadith ni wa Mafuta ya Miski ambayo Abu Said Al Khudhri *RadhiAllahu Anhu* ambae amesema kua: **'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua : Manukato bora zaidi ni Miski.'***(Imam At Tirmidhii)*

Ambapo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na kuikubali Istihalah ya Miski ambayo Damu iliyogeuka na kua Manukato ya Miski.'***(Al Majmuu)*

Ambapo bila ya Shaka Tunapoyaangalia Mafuta mazuri ya Miski basi asili yake kimaumbile hua ni Maji Maji meupe yanayopatikana kutokana na Mnyama aliefanana na Swala ambae hua anaitwa Kulungu Dume Maalum.

Hivyo Miski hua ni Maji maji Mazito meupe yaliyomo ndani ya mfuko wa ngozi uliopo Ndani ya Tumbo la Kulungu baina ya Kitovu chake na Uume wake, na Kulungu husika huyatoa Maji Maji hayo kwa Kukojoa kama yanavyotoka Manii yake. Maji Maji hayo yanapotoka hua ni Meupe na mazito yasiyokua na harufu lakini baada ya kukaa kwa mda na kukauka basi Maji hayo hugeuka na kua na Rangi ya Udongo na kuanza Kutoa harufu nzuri sana ya Miski.Hivyo Miski ni Miongoni mwa Mifano ya Kubadiika kwa Hali moja ya Uharamu wa kitu na kuingia kwenye hali ya Uhalali.

Amesema Al Bunanni kua amesema Al Hafidh Ibn Hajar Al Asqallani kua: '**Damu inayojikusanya kwenye Kitovu cha Paa, Swala au Ngulungu katika wakati maalum wa ndani ya mwaka, hivyo mkusanyiko huo wa Damu unapokusanyika, hua ni wenye kuvimba na kisha Mnyama husika hua ni mwenye kuhisi maumivu, hadi pale donge hilo la Damu ltiakapoanguka(Baada ya Mwezi mmoja tangu kuanza kwake)''** *(Hasyiah Al-Bunani 'ala Hamisi Al-Zurqani*)

Na tunazungumzia kuhusiana na Al Istihalah kwa sababu tunataka kuangalia kuhusiana na Hukmu ya Mafuta ya Nguruwe na Istihalah, jee inakubalika ama la?

Ambapo anasema Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Shirbini Al Shafii kua: '**Wanazuoni wanakubaliana kua Ulevi unapokaa na kuingia katika hali ya Al Istihalah na kugeuka Siki basi hua ni Hala**li.'*(Al Mughni Al Muhtaj)*

Hivyo ingawa Wanazuoni wanakubaliana kuhusiana na hali na Hukmu ya Istihalah katika baadhi ya vitu lakini hata hivyo Wanazuoni hawakubaliani juu ya kukubalika kwa Hali ya Istihalah kwa kila kitu isipokua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhhab ya Imam Malik ambao wao wanasema kua Vitu vyote huweza kua ni tohara pale vitakapoingia katika hali ya Istihalah. Ambapo pia kuna Kauli moja iliyonukuliwa kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahmad juu ya hili.

Ambapo anasema Imam Shihab Ad Din Abu Al Abbas Ahmd Ibn Abi Aala Idris Ibn Abd Rahman Al Qarafi Al Misri Al Maliki Kua: **'*Allah Subhanah wa Ta'ala* ameweka wazi Hukumu ya kua Najis kwa baadhi ya Vitu kwa masharti ya kutokana na kua na Sifa maalum zinazokirihisha**. **Hivyo vyenginevyo Vitu vyote hua ni sawia, na tofauti yao hua ni kulingana na Sifa zao, hivyo kama ikiwa Sifa husika hazipatikani kwenyw kitu husika basi Unajis wa kitu hicho hua ni wenye kukosekana pia, na hii ni kulingana na Makubaliano ya Wanazuon**i.'*(Al Dhakira)*

Na akasema Imam Al Zaylai Al Hanafi kua: **Kwa Upande wa Mtizamo wa Madhhab yetu (Ya Abu Hanifa) basi ni kua Vitu vyote ambavyo ni Najis hua vinatoharika pale vitakapoingia katika hali ya Istihalah**. **Yaani kwa mfano kama Mnyama akitumbukia kwenye Chumvi na akabadilika hadi nae akawa Chumvi, au Kinyesi kinachogeuka na kua Vumbi, au kitakachoungua na kua Jivu, basi hua ji sawa na Ulevi unaogeuka kua Siki**.'*(Tabyin Al Haqaiq)*

Na akasema Imam Ibn Hazim Adh Dhahiri kua: '**Kama kinyesi au Mnyama ameungua na akabadilika na kua Jivu au vumbi, basi Jivu au Vumbi hilo hua Tohara,na linaweza kutumika kwa ajili ya Tayammam.**

Na uthibitisho ni kua hukumu hii ni yenye kutokana na namma *alivyohukumu Allah Subhanah wa Ta'ala*, kulingana na jina la kitu husika, hivyo kama jina la kitu husika likibadilika basi na hukumu yake pia hubadilika, na hivyo hua na hukumu tofauti na aliyoitoa *Allah Subhanah wa Ta'ala* juu ya Kitu husika, kwani Kinyesi hua Si Jivu wala hua si Vumbi kama ilivyokua Pombe si Siki, na Ibn Adam si Damu aliyoumbiwa.'*'*(Al Muhalla)*

Lakini anasema Imam Ibn Al Qayyim Al Hanbali kua: '**Hairuhusiki kwa Kitu kilichokua ni Najis kubakia kua Najis baada ya kubadilika kwa sifa zake na Jina lake. Na hukumu ya kitu husika hua inategemeana na Jina na sifa ya Kitu itakapokuwepo au itakapokosekana pamoja na kitu husika Hivyo Maandishi yaliyoharamisha Mzoga, Damu, Nguruwe na Ulevi hayakujumuisha Mazao, Matunda, Udongo, Chumvi au Siki kimaneno wala kimaana, si kwa kimaandishi wala si kwa kimakisio.'***(Ilam Al Muwaqqi)*

Na akasema Imam Al Mardawi Al Hanbali kua: **'Hakuna kilichokua Najis ambacho hutoharika kwa Istihalah au kwa Moto isipokua Ulevi utakapokua Siki.'***(Al Insaaf Fi Maarifat Rajih min Khilaf)*

Ambapo Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibm Sharaf An Nawawi Al Shafii amesema kua: **'Kuna vitu viwili tu ambavyo hua vinatoharika kutokana na Al Istihalah. Cha kwanza ni Ngozi ya Mnyama itakapookwa Moto, na tumezungumzia juu ya hili katika sehemu yake.**

La Pili ni Ulevi unapokua Siki na hivyo hua unatoharika kutokana na Mabadiliko hayo, kama alivyosema Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu* kua: Asinywe Mtu yeyote Siki iliyotokana na Pombe hadi pale *Allah Subhanah wa Ta'ala* atakapoibadilisha Pombe hio katika kua ni Siki. Yaani hadi Pombe hio iwe Siki kweli kweli, na hapo ndio Siki itakapokua Halali. Hivyo Muislam hua hana kosa pale atakaponunua Siki kutoka kwa Ahl Al Kitab pale itakapokua ana uhakika kua Ahl Al Kitabu hao wamesuburi hadi Pombe hio imegeuka na kua Siki.

Na imehukumiwa hivyo kutokana na Uwezo wake wa kulevya ambao huondoka bila ya kua na uwezo huo, na hivyo hua Tohara.'*(Al Majmuu)*

Ambapo amesema Imam An Nasai kua

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ بَشَّارٍ، حَدَّثَنَا مُعَاذُ بْنُ هِشَامٍ، حَدَّثَنِي أَبِي، عَنْ قَتَادَةَ، عَنْ عِكْرِمَةَ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم نَهَى عَنِ الْمُجَثَّمَةِ وَلَبَنِ الْجَلاَّلَةِ وَعَنِ الشُّرْبِ مِنْ فِي السِّقَاءِ .

Amesema Muhammad Ibn Bashari kua amesema Muadhu Ibn Hisham kua amesema Baba yangu kua Amesema kua Qatadah kua amesema Ikrimah kua amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza Kula Wanyama waliouliwa kwa ajili Kutungia Shabaha, Maziwa ya Mnyama anaekula Kinyesi na Mizoga na Kunywa Kitu kutoka moja kwa Moja kwenye Mdomo wa Vibuyu.'*(Sunnan An Nasai)***

Naam..hii ni moja kati ya Hadith zinazoelezea vitu Vilivyokatazwa kunywewa na kuliwa, ambapo ndani yake mna Wanyama waliowindwa kwa ajili ya kujifunza kutunga Shabaha na Mashindano ya Kutunga Shabaha, yaani kwa ajili ya Starehe na wala si kwa ajili ya Njaa ya Kula.

Pia imekataza Kula Maziwa ya Mnyama anaekula Kinyesi na Mizoga kwani mbali ya kua Nyama ya Wanyama hao imekatazwa lakini pia Maziwa yao yamekatazwa kwa sababu hua Ni Najis pia. Na Pia imekatazwa Kunywa Moja kwa Moja kutoka Mdomo wa Chombo cha Kinywaji kwa sababu ya hatarisho la Maambukizo ya Bakteria wa Mdomo kwenye Chombo cha Maji.

Na tumeanza na Hadith hii kwa sababu hii ni moja kati ya Hadith inayotumika kama uthibitisho wa Wanazuoni kuhusiana na Kutowezekana kutoharika kwa kila kitu kutokana na Al Istihalah. Ambapo kama tulivyoona kua huu ndio Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal na pia Mtizamo wa Imam Abu Yusuf ambae ni Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa hivyo wao wanasema kua:

Najis ya Kitu chengine chochote zaidi ya Ulevi hua haiwezekani kutoharika kwa njia ya Istihalah, kwa sababu Najis hio itabakia tu kwa kula njia katika badiliko la hali ya Kitu hicho. Kwa sababu *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza Kuliwa kwa Nyama na Kunywa Maziwa ya Mnyama anaekula Kinyesi na Najis, kwa sababu Mnyama huyo hua ni Najis, na hiyo kama ingekua kuna Kutoharika kwa Mnyama Huyo kutokana na alichokila kwa njia ya Istihalah basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* asingeharamisha kuliwa.'*(MajmaAl Anhar, Umdat Al Salik, Al Muqni)***

Na kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua**: 'Mtizamo unaotegemewa zaidi na kukubalika katika Madhhab yetu ni kua Najs ya Kitu hua haitohariki kutokana na Al Istihalah.'***(Rawdha Talibin)***

Na huo ndio pia Mtizamo wa Imam Al Khatib Al Shirbini Al Shafii katika kitabu chake cha *Al Mughni al Muhtaj*. Na ndio Mtizamo wa Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Ramli Al Shafii katika kitabu chake cha *Nihayat Al Muhtaj Ila Sharh Al Minhaj*.

Na kwa maana hio basi Madhhab ya Imam Al Shafii hua pia: **'Haikubaliki Kukibadilisha kitu kilichokua Haramu kwa njia ya *Istihalah* kwa Makusudi kwa njia moja au nyeingine ili kitu hicho kibadilike kua Halali.'**

Ambapo Mtizamo huo pia ndio Mtizamo wa Umar Ibn Al Khattab *Radhi Allahu Anhu,* Uthman Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu,* Imam Malik na Imam Ahmad Ibn Hanbal pia.

Na hivyo Ingawa Siku hua ni Halali lakini kama Ulevi utawekwa kwa makusudi ili uwe Siki basi hua Siki hio ni Haram kama alivyosema Imam An Nawawi, Imam Ibn Hajar Al Asqallani, Imam Al Dasuqi, Imam Al Qurtubi, Imam Ibn Al Qayyim, Al Khatib Al Shirbini, n.k.

Lakini kwa Mtizamo mwengine basi tunaona kuna wasemao kua**: 'Kufanya Al Istihalah kwa makusudi kwa ajili ya Kitu kilichoharamishwa ili kukigeuza haki kua Halali hua inakubalika.'**

Na huu ndio Mtizamo wa Abu Dardaa *Radhi Allahu Anhu,* Imam Sufyan Ath Thawry, Imam Al Awzai, Imam Al Layth Ibn Saad, Imam Abu Hanifa baadhi ya Wanazuoni wa Imam Malik na Imam Ahnad Ibn Hanbal pia. Kama alivyosema Imam Al Qurtubi, Imam Ibn Hajar Al Al Asqalani, Al Khatib Al Shirbini na Imam Al Ghanimi pia.

Hivyo kulingana na Mtizamo Unaotegemewa na Madhhab ya Imam Al Shafii na baadhi ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, Imam Ahmad Ibn Hanbal na Mwanafunzi wa Imam Abu Hanifa ambae ni Imam Abu Yusuf Al Hanafi basi ni kua: '**Hukumu ya Hali ya Al Istihalah hua haikubaliki kutumia kwa vitu vyengine vyovyote isipokua vile vilivyotajwa kwenye Mifano ya Aya na Hadith, yaani Istihalah ya Maziwa ya Mnayama ambae ni halali kuliwa, Istihalah ya Ngozi iliyokaushwa, Istihalah ya hali Siki baada ya Ulevi kukaa na kubadilika na kua Siki, na hali ya Istihala ya Manukato ya Miski ambayo ni yenye kutokana na Damu au Majimaji ya mnyama Swala au Kulungu. Ambapo hizi hua Istihalah za aina 4.**

Ambazo ndio zilizotajwa kwenye Vyanzo vikuu vya Asili ya Hukmu za Fiqh yaani Qur'an na Hadith, na hivyo Madhhab ya Imam Al Shafii hayakuruhusu aina nyenginezo zozote za Hukmu ya Istihalah isipokua aina nne hizo.

Na hivyo Kila kitu kinachotokana na Mnyama ambae hajachinjwa kwa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* au aina ya Nguruwe iwe Nyama, Mafuta, Ngozi, Maziwa, Manyoya, Mate yake, Viambatanishi vitokanavyo na Nguruwe, n.k basi hua ni Haram, bila kuangalia kama kimetumika kidogo tu labda kwenye Vyakula vya Makopo, Biskuti, Vipodozi, Shampoo, Sabuni, Chanjo, Mafuta ya Kujipaka, Nyuzi za Kushonea na Brashi za Manyoya ya Nguruwe, n.k.

Na uharamu wake ni kutokana na kua na Asili ya Najis ya Kimaumbile ambayo hua haiwezekani kubadilika hata kwa hali ya Al Istihalah.

Ama tunapozungumzia kuhusiana na vyombo au vitu vitakavyoguswa na Najis ya Nguruwe basi amesema Imam An Nasai kua:

حَدَّثَنَا نَصْرُ بْنُ عَاصِمٍ، حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ شُعَيْبٍ، أَخْبَرَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ الْعَلاَءِ بْنِ زَبْرٍ، عَنْ أَبِي عُبَيْدِ اللَّهِ، مُسْلِمِ بْنِ مِشْكَمٍ عَنْ أَبِي ثَعْلَبَةَ الْخُشَنِيِّ، أَنَّهُ سَأَلَ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ إِنَّا نُجَاوِرُ أَهْلَ الْكِتَابِ وَهُمْ يَطْبُخُونَ فِي قُدُورِهِمُ الْخِنْزِيرَ وَيَشْرَبُونَ فِي آنِيَتِهِمُ الْخَمْرَ . فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " إِنْ وَجَدْتُمْ غَيْرَهَا فَكُلُوا فِيهَا وَاشْرَبُوا وَإِنْ لَمْ تَجِدُوا غَيْرَهَا فَارْحَضُوهَا بِالْمَاءِ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا

Amesema Nasr Ibn Aasim kua amesema Muhammad Ibn Shaybah kua amesema Abdllahi Ibn AlaAi Ibn Zabri kua amesema Abu Uabaid Allah kua amesema Muslim Ibn Mishkami kua amesema Baba yanu kua amesema Abu Thalabah *Radhi Allahu Anhu* kua: Nilimuuliza mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kwa kusema: 'Ya Rasul Allah hakika sisi Tunaishi Na Majirani wa Ahl Al Kitab na hua wanapika Nguruwe kwenye Vyombo vyao na hua wanakunnywa Ulevi, jee tufanyeje?

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Kama Mtapata Vyombo vyengine basi tumieni, lakini kama Mtakosa basi Kosheni vyombo vyao kisha kuleni na Kunyweni.'(Sunnan Abu Daud)***

Ambapo hii ni hadith inayowazungumzia wale watu ambao ni Waislam lakini wanaishi na watu wasiokua Waislam, kwa mfano majirani au labda Mtu alikua Mkristo lakina akasilimu huku akiwa bado anaishi na Wazee wake au Familia yake ambao si Waislam, na pia wale ambao wako Ugenini katika Nchi ambazo kwao wao kupika Nguruwe hua ni kawaida hata katika Mikahawa na Mahoteli n.k.

Na hivyo inakua Vigumu kwa Waislam hao kujiepusha na mazingira hayo. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* katika Hadith hii anabainisha wazi kua '**Kiasili Vyombo vyote hua ni Tohara.**

Na inapotokea hali ya mazingira kama haya kwa Muislam husika basi hua Ni Sunnah kuvikosha Vyombo hivyo kabla ya Kuvitumia.*(Al Qawl Al Mutammad fi Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Na Sunnah hii ni pale itakapokua Mtu hana uhakika kua Chombo husika ndio kilichotumiwa kwa ajili ya kutayarishia chakula chenye Nguruwe huyo. Kwa kama ikiwa Mtu anauhakika kua chombo husika ndio hasa kilichotumika kupikia, kupakulia, kutayarishia n.k Nguruwe basi Hukumu yake hua ni kama ilivyosema hadith iliyotoa hukumu ifuatayo:

وَحَدَّثَنَا عُبَيْدُ اللَّهِ بْنُ مُعَاذٍ، حَدَّثَنَا أَبِي، حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، عَنْ أَبِي التَّيَّاحِ، سَمِعَ مُطَرِّفَ بْنَ عَبْدِ اللَّهِ، يُحَدِّثُ عَنِ ابْنِ الْمُغَفَّلِ، قَالَ أَمَرَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم بِقَتْلِ الْكِلاَبِ ثُمَّ قَالَ " مَا بَالُهُمْ وَبَالُ الْكِلاَبِ " . ثُمَّ رَخَّصَ فِي كَلْبِ الصَّيْدِ وَكَلْبِ الْغَنَمِ وَقَالَ " إِذَا وَلَغَ الْكَلْبُ فِي الإِنَاءِ فَاغْسِلُوهُ سَبْعَ مَرَّاتٍ وَعَفِّرُوهُ الثَّامِنَةَ فِي التُّرَابِ

'Amesema Abdillahi Ibn Muadh kua amesema Baba yangu kua amesema Shu'abat kua amesema Abu Tayyaah kua amesema Mutarrafah Ibn Abd Allah kua amesema Abu Mughafala kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliamrisha Kuwaua (baadhi ya) Mbwa, na akaulizwa kuhusiana wengineo. Ambapo nae akasema: Bakisheni Mbwa wa Kuwindia na wa Kulindia Mifugo yenu.

Na kama Mbwa akiramba Chombo basi kikosheni mara 7 na mara ya 8 sugueni kwa Mchanga.'*(Sahih Muslim)*

Na pia amesema Imam An Nasai kua:

أَخْبَرَنَا عَلِيُّ بْنُ حُجْرٍ، قَالَ أَنْبَأَنَا عَلِيُّ بْنُ مُسْهِرٍ، عَنِ الأَعْمَشِ، عَنْ أَبِي رَزِينٍ، وَأَبِي، صَالِحٍ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " إِذَا وَلَغَ الْكَلْبُ فِي إِنَاءِ أَحَدِكُمْ فَلْيُرِقْهُ ثُمَّ لْيَغْسِلْهُ سَبْعَ مَرَّاتٍ " . قَالَ أَبُو عَبْدِ الرَّحْمَنِ لاَ أَعْلَمُ أَحَدًا تَابَعَ عَلِيَّ بْنَ مُسْهِرٍ عَلَى قَوْلِهِ فَلْيُرِقْهُ

Amesema Ali Ibn Hujri kua amesema Ali Ibn Mus-hir kua amesema Abi Razin na Abu Salih kua amesema Al Amash kua Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: 'Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam kua: Kama Mbwa akiramba Chombo cha Mtu yeyote yule basi na amwage kile kilichomo ndani yake na kisha akikoshe Chombo hicho mara 7.'*(Sunan An Nasai)*

Naam..hizi ni miongoni mwa hadith zinazothibitisha Kua kulingana na Sharia na Hukmu za Kiislam basi ni kua Mbwa ni Najis, na Mate yake hua ni Najis na hivyo tunatakiwa kua Makini na Wanyama hao si katika Vyombo vya kupikia na kulia tu bali katika kila kitu chetu.

Na kama tulivyoona hapo kabla alivyosema Imam Al Faqih Al Aalamah Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii katika Al Hawi Al Kabir kua; '**Nguruwe ni Najis zaidi Kuliko Mbwa Na amesema (Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema) *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameharamisha Mbwa na Bei yao, Ameharamisha Nguruwe na Bei Yao, na ameharamisha Ulevi na Bei Yake Na hii ni kwa sababu Kuweka juu ya Nguruwe bei hua ni Ubaya zaidi kuliko kuweka juu ya Mbwa kwa sababu imekatazwa kunufaika nao katika hali ya mazingira fulani wakati imeruhusika kunufaika na Mbwa katika hali ya Maazingira Fulani.**

Ambapo Unajis wa Mbwa umethibitishwa kam tulivyoona hivyo Unajis wa Nguruwe ndio Unastahiki zaidi'*(Al Hawi Al Kabir fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Na kwa upande mwengine basi aliambiwa Imam Abu Amr Uthman Ibn Abd Rahman Salah Ad Din Al Kurdi Ibn Salah Al Shahrazuri Al Shafii kua: '**Inasemekana kua Wafaransa hua wanatengeneza Kitambaa cha aina ya Jukh (Hariri) kwa kutia Mafuta ya Nguruwe katika wakati wa Utayarishaji wake.**

Ambapo maneno haya wanasema wengi Lakini hakuna aliethibitisha juu yake Jee nini Hukumu yake kuhusiana nayo hii Jukh na Utohara wake?, na Utohara wa kile Kitakachogusana nayo wakati Jukh hio ikiwa imeroa? Kwa mfano kama Njiani n.k? Na pia kuhusina na Ummu al Balwa?.'

Na kabla ya kuendelea basi tukumbushane kuhusiana na hii Ummu Al Balwa, ili kwa wale waliokua hawajuia maana yake au wamesahau basi wakumbuke. Hivyo hapo awali tuliona kua amesema Sulayman Al Bujaraimi Al Shafii kua: **'Ummu Al Balwa hua ni Hukumu ya hali ya mazingira ambayo katika sehemu husika kuna Najis nyingi sana na hivyo hua inakua vigumu kupata sehemu isiyokua na Najis hio katima eneo husika na kupatikana sehemu isiyokua na Najis katika eneo husika humpelekea mtu husika kuingia katika Mashaka makubwa kuipata, hivyo katika hali**

kama hii basi hukumu ya Unajis wa Najis husika hufutika kwa sababu ya kutowezekana kuepukika kwa Najis husika.'*(Hashiyah Al Bujaraimi)*

Hivyo Imam Ibn Salah Al Shafii aliulizwa kuhusiana na Jukh (Hariri) hio kua jee hukumu yake itakua ni sawa na Ummu al Balwa? Yaani inayofutika na kusameheka? Ambapo Imam Ibn Salah Al Shafii nae akajibu kwa kusema kua: '**Kama ikiwa hakuna Uthibitisho wa Kua Jukh hio imetengenezwa kwa Kutumiwa Mafuta ya Nguruwe, na hivyo si Tohara basi hukumu yake ni kua ni sawa na *Ummu Al Balwa* kutokana na kua Unajisi wake huo ambao haujathibitishwa.'** *(Fatawa Ibn Salah)*

Ambapo kwa upande wa Imam Zayn Ad Din Al Malibari Al Shafii basi yeye anasema kuhusiana na Jukh katika Fat-h Al Muin kua: **'Na Jukh ni maarufu kwa kua Utengenezaji wake hua unatumia Mafuta ya Nguruwe, na pia Jibini ya Sham ni maarufu kwa utengenezwaji wake kua ni wenye kujumuisha Mafuta ya Nguruwe.**

Na watu wa Sham walimletea *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Jibini ambapo nae akaila bila ya Kuiuliza juu yake, na hivyo ndivyo alivyosema Shaykh wetu Imam Ibn Hajar Al Haytami katika Sharh Al Minhaj.'*(Fat-h Al Muin)*

Na pia Al Allamah Shaykh Ul Islami Imam Abu Yahya Muhammad Ibn Zakkariyah Al Ansari Al Sunayki Al Shafii amesema kuhusiana na Jukh kua: **'Na Jukh inasifika kutokana na Kutengenezwa kwa kutumia Mafuta ya Nguruwe, lakini ni Tohara'***(Asna Al Matalib)*

Ambapo Fatwa zote hizi zinazungumzia kuhusiana na Jukh kama Mfano wa Kua Ni Kitu kinachosemekana tu kua kimetengezwa kwa Kutumia Mafuta ya Nguruwe, lakini hakuna hata mtu mmoja aliethibitisha hivyo kwa kuona kwa Macho yake. Kwa maana hio basi inapokua hakuna uthibitisho kua kitu husika kimetiwa mafuta ya Nguruwe au viambataniahi vyake basi hukmu ya kitu husika hua ni Tohara kama ilivyo katika Hali ya *Ummu ul Balwa.*

Hivyo tumalizane kuhusiana na Najis ya Nguruwe kwa kukumbushana kua Najis ya Nguruwe hua ni Najis inayojulikana kama *Najis Mughalladhah* yaani Najis Nzito. Ambapo Najis aina hii hua inajumuisha Nguruwe na Mbwa tu. Na hivyo Kulingana na Hadith tulizoziangalia hapo kabla tunaona kua ili Kitu kitoharike kutokana na *Najis Mughalladhah* basi hua ni lazima kukosha kitu husika Mara 7 kitendo ambacho hujulikana kama *Tasbii* ambapo mara moja hua ni lazima Muosho wake uchanganywe na Mchanga ambao pia hujulikana kama *Tatrib.*

Na hivyo ingawa hakuna Hadith iliyosema kuhusiana na Najis ya Nguruwe kua kuondoka kwake basi lazima kitu kikoshwe mara 7 lakini Wanazuoni wametumia makisio ya Kiasi cha Najis ya Mbwa, kwani Najis ya Nguruwe ni nzito zaidi kuliko ya Mbwa kama ilivyoelezewa katika *Fiqh Al Minhaj*.

Na kwa kua Najis *Mughalladhah* inahitajia kuiondoa kwa kukosha kitu mara 7 pamoja na mchanga, basi kitu chochote kile kitakacho ingia Najis Mughalladha hua hakitohariki hadi kikoshwe kwa mfumo hua, yaani kitu hicho iwe Sufuria, Kisu, Sahani, Nguo, Mwili au sehemu kama ilivyosemwa katika *Fiqh Manhaj*.

Kwani amesema Imam Abu Is-haq Al Shirazi Al Shafii kua: '**Amesema Imam Ibn Al Qasim kua: Katika al Qawl Al Qadim imesemwa kua kama Nguruwe akikiramba chombo basi chombo hicho inabidikikoshwe mara moja, na Wanazuoni wenzetu wamesema kua kukoshwe mara 7, na Maneno ya Al Qawl Al Qadim yamesema kua kinatakiwa kikoshwe, na hivyo ilivyomaanishwa ni kua mara 7, nauthibitisho wa hay ani kutokana na kuka Nguruwe ni mbaya zaidi kuliko Mbwa**

kama tulivyoelezea hapo kabla, hivyo ni muhimu kusimamia idadi ya mara 7'*(Al Muhadhdhab fi Fiqh Imam Al Shafii)*

Na ingawa huo ndio Mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Al Shafii lakini pia kuna Mtizamo wa pili ambao hua unakubalika kutumika pale itakapokua Kuna Mashaka ya Kuharibika kitu husika kama Kitakoshwa kwa Tasbi na Tatrib yaani mara 7 na Kusugua kwa mchanga na Maji.

Au labda tuseme kua haiwezekani kukikosha Kitu husika katika hali hio, basi katika mazingira kama haya hua inakubalika kutumia njia aliyoielekeza *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* pale alipoulizwa na Abu Thalabah *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Kutumia Vyombo vya Watu anaoishi Nao wanaokula Nguruwe na kunywa Pombe Ambapo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema kua: Kama mtapata vyombo vyengine basi tumieni, kama mtakosa basi kosheni vyombo vyao kisha tumieni.

Na amesema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Ama kuhusiana na Nguruwe basi Hukmu yake hua ni sawa na Hukmu ya Mbwa kwa kutoharisha kwa kutumia *Tasbii na Tatrib,* ambapo huu ndio Mtizamo Unaotegemewa na kukubalika na ndio Mtizmo wa Mwisho kwenye Madhhab yetu, lakini kwa upande wa Wanazuoni wengine basi wao wana mtizamo wa kua kwa Najis ya Nguruwe basi hua hakuna Ulazima wa kukosha kwa *Tasbii na Tatrib,* ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii, na ushahidi wake ni wenye nguvu hata kwa mtizamo wangu mie.'(***Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo kwa Upande wa Mujaddid Ad Din Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii basi yeye amesema kua: **'Uthibitisho aliouunga mkono Imam An Nawawi Ni unaotokana na Hadith ya Abu Thalabah *Radhi Allahu Anhu.*'***(Talkhis Al Khabir)*

Kwa maana hio basi tunakhitimisha mada kwa kusema kua:

1-Hua ni Wajibu kutoharisha sehemu au kitu kilichonajisika kwa *Najis Mughalladhah* iwe Nguruwe au Mbwa kwa Kutumia Mfumo wa *Tasbii na Tatrib.*

2-Kama ikiwa hakuna Uhakika juu ya Najis husika kama ni *Mughalladhah* ama la basi hua ni Sunnaj kutoharisha kitu au sehemu husika kwa kutumia Maji hadi iondoke athari ya Najis husika.

3-Kama ikiwa ni hakika kua Najis husika ni *Mughalladhah,* lakini kuna hatari au mashaka ya Kuharibika kitu husika kama utatumika mfumo wa kutoharisha kwa *Tasbii na Tatrib* basi inaruhusika kukosha mara moja kwa maji ili kuondoa Athari ya Najis Husika.

MUBTILAT SALAT – NAJIS YA MBWA

❖❖❖❖

Naam..Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallah Alayhi wa Salam* kua:

طَهُورُ إِنَاءِ أَحَدِكُمْ إِذَا وَلَغَ فِيهِ الْكَلْبُ، أَنْ يَغْسِلَهُ سَبْعَ مَرَّاتٍ أُولَاهُنَّ بِالتُّرَابِ

Tohara ya Chombo kinachomilikiwa na yeyote yule miongoni mwenu baada ya Kurambwa na Mbwa, kukikosha mara Saba na kukikosha kwa kutumia Mchanga katika Mara ya kwanza.*'(Sahih Muslim)*

Na anasema Al Imam Al Khatib Shams Ad Din Ibn Muhammad Al Shirbini anasema kuhusiana na Hadith hii kua: '**Dalili ya wazi ya Kutakiwa kutoharisha hua ni sawa na kutoharisha kutokana na Najis nyenginezo, na hivyo hua haimaanishi kua Najis hua ni Chombo husika bali, humaanisha Kukitohariaha chomno kutokana na Kuingia Uchafu wa Najis husika.**

Na hii inathibitisha Unajisi wa Mbwa, na Mdomo wa Mbwa ndio kitu kisafi zaidi katika vitu vya Mnyama huyo Na hivyo vitu vyenginevyo vya Mnyama huyo hua ndio Vina Najis zaidi kuliko Mdomo wake, na hukumu hii pia ndio hivyo hivyo ilivyo kwa Mnyama Nguruwe.' *(Al Iqna Fii Matn Al Faz Abi Shujaa)*

Ambapo kuhusiana na hukumu hii ya Kukosha mara 7 Chombo au kitu kilichorambwa na Mbwa basi Wanazuoni pia wametofautiana kimtizamo juu yake. Kwani kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik Ibn Anas basi wao wanasema kua: **'Kukosha kitu kilichorambwa na Mbwa mara 7 hua ni *Ta'aabudiyah* yaani ni Kuonesha Utiifu wa Amrisho hilo kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam*, lakini hata hivyo Maji yaliyorambwa na Mbwa hua ni yenye kubakia Tohara.'**

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, Imam Muhammad Idris Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: '***Taa'abudiyah* yaani Kuonesha Utiifu hua ni kwa ajili ya Kukosha Mara Saba, lakini si kwa ajili ya Kutoharisha kwani kufanya hivyo hua ni Kutokana na Sababu za Kisharia na hivyo basi Maji yaliyorambwa na Mbwa hua si Tohara.'**

Na hivyo kutokana na kuwepo kwa Utofauti huo basi Wanazuoni wakatofautiana pia katika Wajibu wa kukosha kitu husika mara 7.

Kwani kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik, Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: **'Hua ni Wajibu kukosha kitu Kilichorambwa na Mbwa mara 7, na hii ni kutokana na uthibitisho wa Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*.'**

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua: **'Kukosha Chombo kilichorambwa na Mbwa mara 7 hua si Wajibu bali hua ni Mustahab, yaani kunapendekezwa zaidi.**

Na hii ni kwa sababu Najis ya Mate ya Mbwa hua ni sawa na Najis za aina nyenginezo na hivyo inatosheleza hata kukosha kwa mara moja tu kwa ajili ya kuondoa Najis hio, kwa sababu kuna Hadith nyengine tena ya Abu *Hurayrah Radhi Allahu Anhu* ambayo imenukuliwa na Imam Ad Daraqutni Al Shafii na Imam Al Thalawi.

Ambapo Hadith hio inasema kua Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* alitoa Fatwa kusema kua hua inatosheleza Kukosha mara 3 chombo kilichorambwa na Mbwa, kwa ajili ya kuondoa Najis husika.

Na hivyo kulingana na Mtizamo wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi hii inamaanisha kua kwanza ilikua inapendekezwa kukosha mara 7 lakini kukabatilishwa na Kukosha Mara 3 kulingana na Fatwa ya Abu *Hurayrah Radhi Allahu Anhu*

Hivyo mbali ya kua Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua na Msimamo unasisitiza kua ni Wajibu kukosha mara 7 ikiwemo mara ya kwanza kwa kutumia Mchanga ili kutoharisha Najis inayotokana na Nguruwe na Mbwa na kila kitokanacho nao, na hii ni kutokana na Hadith ya Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* iliyosema kua: **'Tohara ya chombo cha yeyote yule miongoni mwenu baada ya Kurambwa na Mbwa ni kukosha Mara 7 na kwa kutumia mchanga katika Mara yake ya mwanzo.'**(Sahih Muslim)

Ambapo amesema Imam Al Khatim Shams Ad Din Muhammad Al Shiribini Al Shafii kua: '**Ni Wajibu kujitoharisha kwa kujikosha Mara 7 pale Mtu atakapogusana na sehemu yeyote ile ya Mbwa au Nguruwe, iwe kutokana na mate yao, Mkojo wao, au Maji maji yeyote yatokanayo nao Wanyama wawili hawa, na pia sehemu zao kavu za miili yao pale zitakapogusana na kitu kimaji** *(Al Iqna Fii Matn Al Faz Abi Shujaa)*

Ambapo hapo hapo amesema Imam Zayn Ad Din Al Malibari Al Shafii kua: **'Kugusana na Kitu ambacho ni Najis kwa Makusudi hua kitu ambacho Hakikubaliki na kimekatazwa.'***(Fat-h Al Muin)*

Hivyo Mbwa na Nguruwe ni Vitu ambavyo ni Najis Mughallazah ambavyo hairuhusiki kugusana navyo kwa Makusudi bila ya kua na sababu inayokubalika Kisharia. Na Tunapozungumzia kuhusiana na Ilivyoruhusika basi tutafafanua baadae In-shaa Allah.

Na hii kwa sababu Hukmu hii inatofautiana na pale inapokua kuna Dharurah ya Mbwa Husika, yaani kwa mfano Mbwa wa Ulinzi wa Mifugo au Mali, Mbwa wa Kuwindia na Mbwa wanaotumiwa na Vipofu au Askari wa Madawa ya Kulevya na Mbwa wanaosaidia Kutafuta Watu katika Maeneo ya Maafa ya Majanga ya Matetemeko ya Ardhi n.k

Na anasema Imam Wahba Al Zuhayli kua: **'Kila sehemu ya Mnyama Mbwa hua si Tohara kutokana na kua ni mwenye Kujiramba ramba kila mahala katika Mwili wake.'***(Al Mutammad fi Fiqh Al Shafii)*

Ambapo kwa Upande wa Madhhab ya Imam Ahmad Hanbal basi anasema Muwaffaq Ad Din Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: **'Hua Inaruhusika kutumia kitu chengine mbadala wa Mchanga katika Kutoharisha kitu kutokana na Najis ya Nguruwe au Mbwa, kwa Mfano Sabuni Na vitu vyenginevyo kama hivyo.'***(Al Mughni)*

Na pia imesemwa katika *Mawsuah Al Fiqhiyyah Kuwaytiyyah* kua: '**Ama kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi Wao wana mtizamo wa kua Hua si Wajibu kujitoharisha kwa kutumia Mchanga kutokana na Najis ya Nguruwe au Mbwa.'***(Mawsuah Fiqhiyyah Kuwaytiyyah)*

Hivyo mbali ya kua Kuna hadith kadhaa ambazo ni zenye kuthibitisha kua Tohara ya Najis ya kurambwa kitu na Mbwa hua ni Kokosha Mara 7, lakini tumesema kua kwa upande wa Wanazuoni Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi wao wanasema kua inatosha Kukosha mara tatu tu.

Kwani amesema Imam Ahmad Ibn Muhammad Al Tahtawi Al Hanafi kua: '**Na sehemu ya Najis isiyoonekana hua inatakiwa kutoharishwa Mara tatu ambazo hua ni Wajibu na Sunna hua ni mara 7 ambako ndio kumependekezwa kwa Najis ya Mbwa, na hii ni kwa ajili ya kujiepusha ya Kutofautiana na Wanazuoni, na kujizidishia Imani kulingana na Hadith iliyodhahiri.**

Ambapo kulingana na Mtizamo wetu (Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa) basi

Kutoharisha Mara tatu na Kukamua hua hakuna tatizo,lakini si kulingana na Mtizamo wetu, Kwa Mtizamo wetu ni kua Hata Mara moja itatosheleza, kama ilivyosemwa katika Ghayat Al Bayyan, na pia ndivyo ilivyosemwa katika Bahr Al Muhit.

Na kulingana na Mtizamo wa al Musalli basi ni kua hata kama Maji yatapita juu ya Nguo na Mtu akawa na uhakika kua imetoharika basi hua inakubalika na inasihi, hata kama ikiwa haijasuguliwa wala haijakamuliwa kama ilivyosemwa katika *Al Tabyyin na Al Binaa.*

Na katika Al Siraj imesemwa kua Muhimu ni kuhakikisha Kua Imetoharika, ambapo huu ndio Mtizamo unaokubakika zaidi na Watu wa Iraq, na kukadiria kwa mara tatu ni rai iliyotolewa na Bukhari.'(*Hashiyah Al Tahtawi Fii Maraqi Al Falah)*

Ambapo kwa upande wa Maliki Al Ulamaa Imam Alaa Ad Din Abu Bakr Ibn Masud Al Kasani Al Hanafi basi anasema kua: '**Ama kuhusiana na *Najis Al Mughallaza* kama ikiwa haionekani kwa mfano Mkojo n.k, basi hua haiwezekanai kutoharika isipokua kwa kukosha mara tatu.**

Ambapo kulingana na Mtizamo wa Imam Al Shafii basi ni kua nguo hua inaweza kusafishwa hata mara moja tu kwa kulingana na Najis husika isipokua katika kesi ya Kurambwa na Mbwa, hii inatokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua:

طَهُورُ إِنَاءِ أَحَدِكُمْ إِذَا وَلَغَ فِيهِ الْكَلْبُ، أَنْ يَغْسِلَهُ سَبْعَ مَرَّاتٍ أُولَاهُنَّ بِالتُّرَابِ

Mbwa akiramba chombo cha mmoja wenu basi na akikoshe mara 7, mara moja iwe kwa Mchanga.

Na vile vile sisi tunayo hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: Chombo kikoshwe mara 3 baada ya Mbwa kukiramba, hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha kua kikoshwe mara 3.

Na alichozungumzia Al Shafii ni hukumu ya mwanzoni mwa Uislam, ambayo ilikua na malengo ya kuwafanya watu waachane kua na Urafiki na Mbwa. Yaani sawa na ilivyoamrishwa na kuvunjwa kwa vyombo vya Ulevi ulipokatazwa Ulevi, na hivyo watu walipoacha kulewa basi amrisho hilo likaondolewa.

Hivyo katika hili la Mbwa pia imaashiria hivi pale ilipoamrishwa Kukosha Mara 7 na mchanga Mara moja, kama ilovyosemwa katika Hadith, jambo ambalo hua si Wajibu, kulingana na Makubaliano.' *(Badai Al Sanai)*

Imam Al Kasani anaendelea kufafanua kwa kusema kua: '**Na pia imepokewa kutoka kwake *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kusema kua: 'Mmoja wenu akiamka Kutoka Usingizini basi na asichovye mkono wake kwenye chombo cha Maji hadi aukoshe mara 3, kwani hajui mkono wake huo ulipita wapi katika wakati wake wa Usiku. Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* ameamrisha kukosha Mara tatu inaposhukiwa kua kuna Najis, na kawa maana hio basi Mtizamo wa kukosha mara Tatu ni wenye nguvu zaidi, na kwa sababu Najis hata kwa mara moja huweza kuondoka.**

Na maandiko yamesema kua Kukosha Mara moja kunatosha, kwa sababu hata *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alitia Udhu mara moja moja tu kwa kila kiungo na kisha akasema kua: 'Huu ndio Udhu ambao *Allah Subhanah wa Ta'ala* haikubali Sala ya Mtu bila kutokana nao. Na

hivyo Kutia Udhu mara tatu kwa kila kiungo hua si lazima, bali kunapendekezwa tu.'*(Badai Al Sanai)*

Naam..baada ya kuangalia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa kuhusiana na namna ya Kujitoharisha kutokana na *Najis Mughallazah* yaani Najis nzito ya Nguruwe na Mbwa, kwa Kukosha kitu hata Mara tatu tu hua hamna tatizo ambao ni mtizamo uliotofautiana na Mitizamo ya Madhhab mengineyo yenye kusimamia kukosha kitu husika mara 7 kua ni Wajibu.

Na pia kuona kua ni Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii tu ndio waliosimamia Mtizamo wa kua ni Lazima mara moja iwe ni kwa kukosha kwa mchanga. Ambapo Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Hanbal basi wao wamesema kua Inakubalika kutumia kitu mbadala ya Mchanga kwa mfano Sabuni. Na kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Imam Malik basi wao wanasema kua kukosha kwa Mchanga hua si Wajibu.

Ambapo kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii na wote wanaosimamia kwenye Mtizamo wa Kua Kukosha Kwa Mchanga hua ni wajib basi wao wanahoja zifuatazo:

1-Hadith zimesema Mchanga hivyo hua kuna Wajibu wa Kufuata Uthibitisho wa Hadith kiushahidi katika Hukumu.

2-Katika Wakati wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ilikua Kuna vitu kama Sabuni ambavyo vilikua vikitumika kufulia na kukoshea lakini hata hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* hakuvitaja, bali alisema moja kwa moja kua ni Mchanga.

3-Kua Hikma iliyomo katika Hukumu ni kua Inawezekana katika Mchanga kuna vitu ambavyo vinaweza kuua Vijidudu vinavyosababisha Madhara na hivyo kua ni Najis ndani ya Mate ya Mbwa.

4-Mchanga hua unakubalika kutumika kama Kitahirisho sawasawa na Maji pale yanapokosekana Maji kwa mfano katika Tayammam, lakini Sabuni na vitu vyenginevyo vinavyofanana na Sabuni hua havikubakiliki kua mbadala wa Kitoharisho.

Na kwa upande mwengine basi tunapoangalia zaidi basi tunaona kua Wanazuoni wa Karne yetu Kwa Mfano katika Moja kati ya Fatwa za Chuo Kikuu cha Al Azhar cha Misri ambacho ni chenye Wanazuoni ambao ni wafuasi wengi zaidi wa Madhhab ya Al Shafii, kiasi ya kua tangu kuanzishwa kwake basi Asilimia 90 ya Mamufti Wakuu wake hua ni Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi wamesema kua: **'Inapendekezwa zaidi kutumia Mchanga kwa ajili ya Mkosho wa kwanza dhidi ya Najis ya Mbwa au Nguruwe, na hii ni kutokana na Uthibitisho wa Hadith.**

Lakini hata hivyo hua pia Inaruhusika Kutumia Kitu mbadala wa Mchanga kama kitoharisho katika wakati wetu kama kitu hicho kikiwa kinaweza kutoharisha, kwa sababu kinachotakiwa hua ni Kutoharika kulingana na Hukumu za Sharia.'*(Dar Al Ifta Masriyyah)*

Na kwa upande mwengine basi tunapoangalia pia Kamati ya Fatwa ya Wanazuoni wa Kiislam wa Malaysia ambao pia ni Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi nao wamesema kua: '**Hua inakubalika kutumia Sabuni zenye kutiwa na Udongo laini ndani yake katika Kutengenezwa kwake kwa ajili ya Kujitohariaha na Najis Mughallazah, pale itakapokua Udongo huo ni Tohara, na asilimia ya Udongo huo ni kubwa zaidi ya vitu vyengine vilivyotumika katika kutengenezwa Sabuni husika vyenye kuruhusika Kisharia**.' *(Muzakarah Al Fatawa Malaysia)*

Kwani kama tulivyoona kulingana na Hadith kua ni jambo la Dhahir kua Mbwa ni Najis, na ingawa Hadith zimezungumzia Mate ya Mbwa lakini kutokana na kua ni Najis ya Mbwa ni *Najis Mughallazah* basi Wanazuoni wamehitimisha kua sehemu nyenginezo zote za Mbwa hua ni Najis, yaani Jasho lake, Manyoya yake, Ngozi yake, na kila kitu chake na hii ni kutokana na Kupenda kujiramba kwake.

Na tumeona kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam:*

طَهُورُ إِنَاءِ أَحَدِكُمْ إِذَا وَلَغَ فِيهِ الْكَلْبُ، أَنْ يَغْسِلَهُ سَبْعَ مَرَّاتٍ أُولَاهُنَّ بِالتُّرَابِ

Tohara ya Chombo cha mmoja wenu miongoni mwenu kitakachorambwa na Mbwa basi ni kusafishwa kwa maji mara 7 na mara ya kwanza kwa Mchanga.*(Sahih Muslim)*

Na kuhusiana na Muosho wa Mchanga basi kuna Hadith aliyoinukuu Imam At Tirmidhii ambayo inasema:

يُغْسَلُ الإِنَاءُ إِذَا وَلَغَ فِيهِ الكَلْبُ سَبْعَ مَرَّاتٍ: أُولَاهُنَّ أَوْ أُخْرَاهُنَّ بِالتُّرَابِ

Kosheni mara 7 Chombo kilichonywewa Maji yake na Mbwa, na Kosho la Mwanzo au La Mwisho liwe la Mchanga.'*(Sunnan At Tirmdhii)*

Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii anasema kuhusiana na amrisho hili kua: **'Hadith zilizotumia neno *'Awlahuna bi Al Turabi* - (Kosho) La Mwanzo kwa Mchanga.' ni zenye nguvu zaidi kutokana na wingi wake na zimehifadhiwa Zaidi. Na pia Maana ya Hadith hizi inaonesha kua Kama ikiwa kosho la Mwisho ndio liwe la Mchanga basi lazima kutahitajika kosho moja zaidi ili kukamilisha Tohara na Usafi wa Kuondoa Mchanga.'***(Fat-h Al Barr)*

Hivyo suali la kujiuliza ni kua Kwanini Iwe lazima kwa Turabi au Mchanga?

Na tunapoangalia neno *Turabi* basi tunaona kua kilugha hua linatokana na neno *Tariba* ambalo humaanisha Kua na Mchanga mwingi, Kujaa Mchanga, Kua na Michanga Mikononi na pia humaanisha kua na Hali mbaya ya kutokua na Kitu au ya kutokua na uwezo wa kupata Mahitajio.

Neno *Tariba* ndio lililotoa neno *Tirb* yaani Mtu mwenye kufana na mwenzake katika mambo na vitu avipendavyo.

Na pia likatoa neno *Taraib* linalomaanisha Kifua Mbavu na pia humaanisha Maziwa au sehemu za juu za Kifua cha Mwanammke kama zilizvyosema aya:

﴿فَلۡيَنظُرِ ٱلۡإِنسَانُ مِمَّ خُلِقَ ۝ خُلِقَ مِن مَّآءٖ دَافِقٖ ۝ يَخۡرُجُ مِنۢ بَيۡنِ ٱلصُّلۡبِ وَٱلتَّرَآئِبِ﴾

Falyandhuri al-insanu mimma khuliqa; Khuliqa min ma-in dafiqin Yakhruju min bayni alssulbi waalttara-ibi.*(Surat At Tariq 86:5-7)*

Tafsir: **Hebu Na Ajiangalie Mtu ameumbwa Kutokana na nini? Ameumbwa Kutokana na Maji yatokayo kwa Mchupo Yatokayo Baina ya Uti wa Mgongo na Kifua, Mbavu.**

Hivyo Neno *Tariba* ndio lililotoa neno *Turab* ambalo humaanisha Mchanga Mwepesi, Vumbi au sehemu ya Juu ya Ardhi.

Na tunapouangalia Mchanga ambao ni moja kati ya vitu vilivyoruhusika kujitoharishia kama tulivyofafanua kwenye Tayammam basi tunaona kua kimaumbile Mchanga ni Kitu chenye sifa ya kua ni Kinga dhidi ya Bakteria na *Antibiotic* na pia una sifa ya kuzuia ukuaji na usambazaji wa Fangas na Bakteria kama aina ya *Staphylococcus, Eschericia Coli, Salmonella Typhi* na *Enterobacter Aerogenes.* Na hii ni kwa sababu Mchanga hua unabeba aina tofauti za asilimia za Madini yakiwemo Madini ya *Chuma, Zinc, Shaba na Nickel.*

Na unajumuisha pia Asilimia tofauti za *Antibiotic* yenye kubeba Bakteria, Fungi na Protozoa wanaohitajika mwilini, Mchanga unabeba *Antibiotic* pia inayojulikana kama *Malacidin* ambayo ni *Antibiotic* inayotumika katika kutibu maradhi yanayosababishwa na usugu wa mwili dhidi ya Madawa na Wadudu Sugu wa Maradhi watakaoingia mwilini kama *Staphylococcus Aureus*.

Kwani hawa Bakteria Sugu wa aina ya *Staphylococcus Aures* ndio wanaopatikana kwenye Mate ya Mbwa, yakiwa pamoja na Bakteria waitwao *Dipylidium Caninum, Escherichia Coli, Echinococcua na Salmonella Typhi.* Na pia baadhi ya Mate ya Mbwa hua na Bakteria waitwao *Capnocytophaga Canimorsus* ambao huweza kusitisha ufanyaji kazi wa baadhi ya Viungo Muhimu vya ndani ya Mwili wa Ibn Adam.

Na bila ya Shaka Wanasayansi wa Chuo Kikuu cha Kiislam cha Malaysia wamefanya Utafiti na kugundua kua Mate ya Mbwa yanaposafishwa Mara 7, mara ya kwanza kwa Mchanga basi athari ya Bakteria wanaodhuru kwenye Mate hayo hutoweka kwa asilimia 99% hadi 100% kulingana na Aina za Mchanga Tofauti.

Hivyo Kukosha Mara 7 na kwa Mchanga kitu alichokiramba Mbwa hua kunakitoharisha kabisa na hivyo hii ni Moja kati ya Miujiza ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam.*

Na amesema Al Marhum Shaykh Yusuf Al Qardhawi kua: **'Unakuta katika Jamii zetu kuna Watu ambao wanaiga Mambo ya Kimagharibi, na kuchukulia kua Watu wa Magharibi wana ukarimu na upole hususan kwa kila ya aina ya Wanyama,na hivyo kuwashutumu Waislam kua ni wenye kua na Tahadhari na Wanyama wanaowafuga ambao ni wenye kuvutia.**

Hivyo Ujumbe huu ni kwa ajili ya wale Wanaowaamini sana Wanyama, kwani kuna Profesa wa Kijerumani aitwae Dr Gerrard Fantestimmer ambae ametahadharisha juu ya Hatari ya Ufugaji Mbwa Majumbani au kua na Ukaribu sana nao.

Kwani kwa hakika Idadi ya Wafugaji Mbwa imeongezeka jambo ambalo linatupekelekea sisi kutoa Tahadhari zinazosababishwa na Si Kuwajali tu Mbwa bali pia na Kupenda kucheza nao, Kubusiana nao,na kuwaruhusu kuramba Mikono na Miguu hata ya Watoto wetu Wadogo wachia mbali Watu wazima, na baadhi kufikia kuwaruhusu hata kuramba Vyombo vyao vyenye Vyakula ndani yake.

Na ingawa kufanya hivyo hua kunakirihisha kulingana na Maumbile ya Kiibinadam, lakini pia hua ni Jambo linalopingana na Kanuni za Kiafya Kulingana na Mtizamo wa Kitabibu basi jambo hilo hua haliwezi kudharaulika kwani linahatarisha maisha ya Ibn Adam.

Na kutokana na kua Ibn Adam ni wakaidi na ni wenye kujitolea kutumia Pesa Nyingi kwa ajili ya Kuwasimamia Mbwa wanaowafuga, hivyo badala yake Wanyama hawa wamekua ni wenye

kuzalisha Wadudu hatari wanaoweza kusababisha Maradhi Sugu na ya Mda mrefu na huweza kusababisha Kifo kwa baadhi ya Watu.

Kwa mfano Minyoo Mirefu iliyomo ndani ya Mate ya Mbwa hua ni wenye kuambukiza na kusababisha Mapele, na pia huweza kuambukiza Wanyama wengine pia kwa hususan Nguruwe na Mbwa Mwitu, na hua ni Nadra kuambukizika kwa Paka.

Na Maumbile ya Minyoo hio hua ni Vigumu sana kuonekana kwa Macho, kwani hata kugundulika kwenyewe imegundulika karibuni tu.

Ambapo Ukuaji wa Minyoo hio itokanayo na Mbwa hua ni wa upekee kwa sababu Yai la Mnyoo mmoja tu linatoa Minyoo kadhaa, na hivyo hua ni yenye kuzaliana kwa wingi ndani ya Tumbo la Mbwa.

Ambapo Ukuaji wake ndani ya Mwili wa Wanyama wengine pamoja na Ibn Adam hua haukui zaidi ya Maumbile yake, ingawa kwa nadra huweza kukua kwa Ukubwa mkubwa zaidi ukiwa na Maji maji ya rangi ya Njano na huyaathiri Maini, na kisha pia huhamia katika Mapafu, Mafigo na Viungo vyengine ndani ya Mwili hadi Ndani ya Kichwa huku ikiwa ni yenye kubadilika kitabia na kimaumbile.

Na Hadi sasa bado haijagundulikana Njia ya Kujikinga kutokana na Maambukizi yake Minyoo hio. Ambapo anasema Professor Dr Noveller ambae ni Mtaalamu wa Upasuaji wa Ujerumani kua Watu waliokutwa na Matatizo ya Minyoo hio .

Nchini Ujerumani hua hawazidi asilimi 1%, ambapo Idadi kubwa zaidi ya wenye matatizo ya Minyoo hio ni watu wa Skandinavia na Watu wa Kusini Mashariki mwa Australia, ambapo nchini Ireland basi katika kila watu 43 basi Mmoja wao ana Matatizo ya Minyoo hio.

Hivyo kama Ikiwa Ibn Adam tutachunguza upotezwaji wa Maisha ya Watu kutokana na Wadudu wa Maradhi yatokanayo na Mbwa basi bila ya shaka hakuna hata mmoja miongoni mwetu angelikua ni mwenye kupinga kuuliwa kwa Mbwa Duniani kwa ajili ya Kupata Usalama wa Watu.

Hivyo Jambo bora kwetu katika kupigana vita na Maradhi yatokanayo na Mbwa basi ni kuwaachia Mbwa wawe kivyao bila ya kua na ukaribu nao, jambo ambalo haliwezekani kwa sababu haiwezekani kuwazuia Watu kujitenga na Wanyama hawa.

Ambapo hii inadhihirisha sababu kuu juu ya kwanini *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaruhusu Kufuga Mbwa kwa Dharurah tu na kutuonya kutokua na ukaribu nao, kwa sababu ya kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni mwenye Kujali Afya za Watu' *(Al Halal Wa Al Haram Fi Al Islam)*

Kwani kuna suali ambalo baadhi miongoni mwetu wanaweza wakajiuliza ambalo linasema kua: Jee kwa Mfano imetokezea kua Mtu ameenda Ugenini labda katika Makazi ya Wasiokua Waislam na akakoga, na kisha baada ya Kukoga akagundua kua Sabuni aliyotumia imetengenezwa na Mafuta ya Nguruwe.

Au amekaribishwa Nyama na baada ya kula akagundua kua niNyama ya Nguruwe au ya Mbwa Au Labda amekaa sehemu na mara akatokezea Mbwa akamramba n.k. Jee hukumu yake ni zipi juu ya mambo haya?

Hivyo tunapoangalia *Al Mughni Al Muhtaj* ya Imam Shams Ad Din Muhammad Al Khatib Al Shirbini Al Shafii anasema kuhusiana na Mtu ambae ameoa Mwanamke wa Ahl Al Kitab ambae amekula Nyama ya Nguruwe kua: '**Kuna MitIzamo miwili kuhusiana na Mwanamke Husika ambapo kwanza ni kua hua anatakiwa akoge aidha kwa Kukoga mara 7 na mara moja kwa Mchanga Na mtizamo wa pili ni kua Mwanamke husika anatakiwa akoge mara moja tu na bila ya kutumia mchanga. Ambapo hata hivyo Mtizamo ninaoupendelea zaidi ji wa kwanza.'** *(Al Mughni Al Muhtaj 4/314)*

Ambapo mtizamo huo pia ndio Mtizamo wa Imam Al Sharwani Al Shafii katika Hawashy Tuhfah Al Muhtaj 7/319.

Ambapo ingawa huo ni Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii lakini hata hivyo kama itakua haiwezekani kukoga mara 7 pamoja na Mchanga basi hua inakubalika kufuata Mtizamo wa Mujaddid Ad zdin Mujtahid Imam Imam Muhammad Idris Al Shafii mwenyewe ambao pia ndio Mtizamo alioupendelea Shaykh ul Islami Imam An Nawawi ambao ni Mtizamo wa Ikhtiyar wa kukoga Mara moja tu.

Na pia kama itakua vigumu kukoga kwa kutumia Mchanga pia basi kuna Mtizamo mwengine wa Imam Al Shafi usemao kua inaruhusika kutumia Sabuni na vitu kama hivyo badala yake kama alivyosema tena Imam Al Khatib Al Shirbini kua **'Imeelezewa pia kua inaruhusika kutumia kitu chenginecho, pale itakapokua Mchanga utasababisha Madhara juu ya kile kinachotakiwa kutoharishwa kwa mfano Nguo, hivyo kulingana na Mtizamo mwengine wa Imam Al Shafii (Muqabil Al Azhar) basi inaruhuisika kutumia kitu chengine badala ya mchanga.**'*(Al Mughni Al Muhtaj)*

Hivyo tunapoangalia katika Madhhab ya Imam Al Shafii basi tunaona kua kuna Mtizamo Mitano iliyonukuliwa juu ya haya ambayo ni:

1-Mtizamo unaokubalika zaidi juu ya Nguruwe ni kua kuna Ulazima wa kukikosha kitu mara 7, mara ya mwanzo kwa mchanga kutokana na Najia yake.

2-Kuna Mtizamo ambao unaweza kutumika ambao ni kua Kitu husika lazima kikoshwe mara 7, na inakubalika kutumia kitu mbadala ya mchanga kwa mfano Sabuni.

3-Kuna Mtizamo ambao pia unakubalika kutumika ambao ni kua Inakubalika Kukikosha kitu husika mara 7, na kama utakosekana mchanga basi inawezekna kutumia kitu mbadala kama sabuni.

Ambapo tofauti kati ya Mtizamo wa pili na huu wa tatu ni kua Mtizamo wa 2 ni kwamba hata kama Mchanga upo basi unaweza kutumia Sabuni. Na Mtizamo wa 3 ni kua Kitatumika kitu mbadala pale utakapokosekana Mchanga.

4-Kuna Mtizamo ambao unaweza kutumika wa Kukikosha kitu mara 7 na Kutumia kitu mbadala wa Mchanga yaani kama sabuni pale itakapokua Mchanga unaweza kusababisha Madhara.

Ambapo Mtizamo wa kwanza hadi wa Nne hua ni kwa ajili ya Kutoharisha Mwili au kitu chengine kutokana na Najis ya Mbwa au Nguruwe.

5-Kuna Mtizamo ambao ni wa Imam Al Shafii Mwenyewe kua Itatosheleza kusafisha kitu husika japo mara moja tu, lakini Mtizamo huu unahusiana na Najis ya Nguruwe tu, kwani hauhusiani na Najis ya Mbwa.

MUBTILAT SALAT – JEE INARUHUSIKA KUFUGA MBWA

❖❖❖❖

خْبَرَنَا عَلِيُّ بْنُ حُجْرٍ، قَالَ حَدَّثَنَا إِسْمَاعِيلُ، - يَعْنِي ابْنَ جَعْفَرٍ - قَالَ حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ أَبِي حَرْمَلَةَ، عَنْ سَالِمِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، عَنْ أَبِيهِ، قَالَ قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم " مَنِ اقْتَنَى كَلْبًا إِلاَّ كَلْبَ مَاشِيَةٍ أَوْ كَلْبَ صَيْدٍ نَقَصَ مِنْ عَمَلِهِ كُلَّ يَوْمٍ قِيرَاطٌ " . قَالَ عَبْدُ اللَّهِ وَقَالَ أَبُو هُرَيْرَةَ " أَوْ كَلْبَ حَرْثٍ ".

Amesema Ali Ibn Hujar kua amesema Ismail yaani Ibn Jafar kua amesema Muhammad Ibn Abi Harmallah kua amesema Salim Ibn Abd Allah kua amesem Baba yake kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaefuga Mbwa asiekua wa Kulindia Mifugo yake au Ardhi au wa Kuwindia yake basi atapunguziwa Malipo ya amali zake njema kwa Qirat mbili kwa kila siku. Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua au Mbwa wa Shambani.' *(An Nasai)*

Na anasema Imam Muslim Ibn Hajaj kua:

حَدَّثَنَا يَحْيَى بْنُ يَحْيَى، وَيَحْيَى بْنُ أَيُّوبَ، وَقُتَيْبَةُ، وَابْنُ، حُجْرٍ قَالَ يَحْيَى أَخْبَرَنَا وَقَالَ الآخَرُونَ، حَدَّثَنَا إِسْمَاعِيلُ، عَنْ مُحَمَّدٍ، - وَهُوَ ابْنُ أَبِي حَرْمَلَةَ - عَنْ سَالِمِ بْنِ عَبْدِ، اللَّهِ عَنْ أَبِيهِ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " مَنِ اقْتَنَى كَلْبًا إِلاَّ كَلْبَ مَاشِيَةٍ أَوْ كَلْبَ صَيْدٍ نَقَصَ مِنْ عَمَلِهِ كُلَّ يَوْمٍ قِيرَاطٌ " ". قَالَ عَبْدُ اللَّهِ وَقَالَ أَبُو هُرَيْرَةَ " أَوْ كَلْبَ حَرْثٍ

Amesema Yahya Ibn Yahya kua amesema Yahya Ibn Ayoub Ismail kua amesema Qutaybah kua amesema Ismail kua amesema Muhammad ambae ni Ibn Abi Harmalah kua amesema Salim Ibn Abd Allah kua amesem Baba yake kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Yeyote yule atakaefuga Mbwa asiekua wa Kulindia Mifugo yake au Ardhi au wa Kuwindia yake basi atapunguziwa Malipo ya amali zake njema kwa Qirat mbili kwa kila siku. Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua au Mbwa wa Shambani.' *(Sahih Muslim)*

Na kuna Hadith isemayo kua:

وعن أبى هريرة رضى الله عنه قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم : "من أمسك كلبًا فإنه ينقص كل يوم من عمله قيراط إلا كلب حرث أو ماشية" ((متفق عليه)).

Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua; 'Atakaefuga Mbwa basi atapoteza Qirat moja kutoka katika Malipo ya Amali zake njema za Kila siku, isipokua yule ambae atakaemfuga kwa ajili ya Kulindia Shamba lake au Mifugo yake' *(Mutaffaq Alayhi)*

Ambapo wanakubaliana Wanazuoni kua Hadith hizi zinathibitisha kua ni Haramu Kufuga Mbwa bila ya Kua na Sababu Maalum, kwani kufanya hivyo hua ni Kujipunguzia Malipo ya Amali njema za Ibada ya Mtu husika katika Kila siku yake anayoishi na Mbwa hao. Na punguzo hilo hua ni Qirat Mbili, ambazo kipimo chake kinajulikana na *Allah Subhanah wa Ta'ala* peke yake.

Na Mujaddid Ad Din Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii anasem akuhusiana na hadith hii kua '**Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na maana ya Qirat katika hii, kwani kuna wanaosema kua hua ni sawa na maana ya Qirat kilichotajwa katika Hadith inayozungumzia kuhusiana na Malipo ya Mtu atakeenda Mazikoni na kumsalia na Kumzika maiti husika wa Kiislam kua ni sawa na Ukubwa wa Mlima wa Uhud, hivyo kuna wanaosema kua Qirat cha Hadith hii ya Mbwa hua ni sawa na Qirat cha Hadith hii ya Maziko.**

Na Wengine miongoni mwa Wanazuoni basi wao wanasema kua kuna maana tofauti kwani Qirat kilichotajwa kwenye Hadith ya Maziko kinaainisha Manufaa wakati Qirat kilichotajwa katika Hadith ya Mbwa kinaainisha Hasara.'*(Fat-h Al Barri bi Sharh Sahih Al Bukhari)*

Kwani anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Hadith hii inathibitisha kua Malipo ya Thawabu za Amali njema za Mtu hua zinapunguzwa kila siku wakati akiwa anamfuga Mbwa huyo. Lakini hata hivyo Kufuga Mbwa kwa ajili ya Kuwindia, Ulinzi wa Shamba, Mifugo n.k hua inaruhusika, kwani amesema Al Shafii na As-habi wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua: 'Hairuhusiki Kufuga Mbwa bila ya kua na sababu Maalum Inayokubalika Kisharia kama vile Kuwafuga kwa ajili ya Ulinzi wa Mifugo, Mazao au Kuwindia, na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wote wanakubaliana juu ya hilo.''***(Al Majmuu)***

Ama Kwani kwa upande mwengine basi kuna Hadith isemayo kua:

وَاعَدَ رَسولَ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وَسَلَّمَ جِبْرِيلُ عليه السَّلَامُ في سَاعَةٍ يَأْتِيهِ فِيهَا، فَجَاءَتْ تِلكَ السَّاعَةُ وَلَمْ يَأْتِهِ، وفي يَدِهِ عَصًا، فألْقَاهَا مِن يَدِهِ، وَقالَ: ما يُخْلِفُ اللَّهُ وَعْدَهُ وَلَا رُسُلُهُ، ثُمَّ التَفَتَ، فَإِذَا جِرْوُ كَلْبٍ تَحْتَ سَرِيرِهِ، فَقالَ: يا عَائِشَةُ، مَتَى دَخَلَ هذا الكَلْبُ هَاهُنَا؟ فَقالَتْ: وَاللَّهِ، ما دَرَيْتُ، فأمَرَ به فَأُخْرِجَ، فَجَاءَ جِبْرِيلُ، فَقالَ رَسولُ اللهِ صَلَّى اللَّهُ عليه وَسَلَّمَ: وَاعَدْتَنِي فَجَلَسْتُ لكَ فَلَمْ تَأْتِ، فَقالَ: مَنَعَنِي الكَلْبُ الَّذي كانَ في بَيْتِكَ؛ إنَّا لا نَدْخُلُ بَيْتًا فيه كَلْبٌ وَلَا صُورَةٌ..

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alikua na miadi na Malaika Jibril Alayhi Salam kua akutane nae Lakini hata hivyo ulipowadia Mda waliokubaliana kwa ajili ya miadi hio basi Malaika Jibril hakuja.**

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae alikua na Fimbo, basi aliitupa chini fimbo hio na kusema: 'Hakika Allah havunji miadi yake wala Mitume wake.'

Na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salaam* akageuka na mara akaona Mbwa mdogo chini ya Kitanda chake, hivyo akasema: Ya Aisha! Ni Wakati gani huyu Mbwa aliingia Humu ndani? Aisha *Radhi Allahu Anha* akasema: 'Wa Allahi mimi hata Sijui!'

Hivyo *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamrisha kua Mbwa huyo atolewe nje. **Na kisha Malaika Jibril akatokea na akasalimiana na *Rasul Allah Salallahu Alayhu wa Salam, na Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akamuuliza Malaika Jibril kwa kusema: Ya Jibril hakika wewe uliniahidi mimi kua utakuja, nami nikakusubiri lakini hukutokea.**

Hivyo Malaika Jibril akasema: Mbwa aliekuwepo ndani ya Nyumba yako alinizuia mimi kuingia Ndani yake, kwa sababu sisi hatuingii katika Nyumba yenye Mbwa au yenye picha yake.'*(Sahih Muslim)*

Na Shaykh Ul Islami Muhyi Ad Din Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii anaielezeakwa kuifafanua Hadith hii kwa kusema kua: **'Sababu zinazowafanya Malaika wasiingie Ndani ya Nyumba yenye Mbwa ni zifuatazo:**

1-Mbwa hua wanakula Najis.

2-Baadhi ya Mbwa wamenasibishwa na Shaytani katika baadhi ya Hadith na Malaika hua hawapatani na Shaytani.

3-Mbwa hua wana harufu mbaya na Malaika hua hawapendi Harufu mbaya.

4-Kuna Katazo la Kutofuga Mbwa, hivyo Mtu atakaefuga hua anaadhibiwa na Malaika wenye kueneza Barka ardhini kaa kutoingia ndani ya Nyumba yake.'*(Sharh Sahih Muslim)*
Lakini hata hivyo hii hua haimaanishi kua Malaika Raqib na Atid wanaomuandikia Kila Mtu amali zake hua hawaingii ndani ya Nyumba ya Mhusika, la! Kwa Sababu Malaika hawa hua wanaenda nae kila mahala kwa ajili ya kuandika amali zake njema na ovu. Hivyo Malaika wanaozungumziwa hapa ni Malaika wenye kuleta Rehma, Baraka na Kumuombea Dua Mtu hua hawaingii ndani ya Nyumba yenye kufugwa Mbwa.

Hivyo hii kukosekana kwa Dua, Rehma, na Maghfira ya Malaika kwa watu wa Nyumba husika hua ni Adhabu tosha, wacha mbali hio kufutiwa Thawabu zenye Thamani ya kutoa Sadaka ya Dhahabu yenye Ukubwa wa Milima miwili ya Uhud.

Hivyo bila ya shaka kufuga Mbwa bila ya kua na sababu Maalum hua ni Kujiangamiza.Hivyo ingawa Kiislam hua hairuhusiki kufuga Mbwa bila ya Kua na sababu maalum inayokubalika kisharia, yaani Mbwa huyo awe ni kwa Maslahi ya kuleta Manufaa kwa Mtu husika, Kwani amesema Al Faqih Al Allamah Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii kua: **'Hukumu juu ya Kufuga Mbwa ni kua Kiislam hua Hairuhusiki, isipokua pale itakapokua kuna Manufaa katika Ufugaji huo, hivyo kama itakua kuna manufaa basi itaruhusika.'***(Al Hawi Al Kabir)*

Kama tunavyoona kua kwa Upande wa Madhhab ya Imam Al Shafii basi anasema Shaykh Ul Islami Imam Ahu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**Kuna Utofauti wa Mitizamo kuhusiana na kua kama inaruhusika Kufuga Mbwa kwa sababu ya zaidi ya Tatu tofauti na hizi zilizotajwa kwenye Hadith hii, na mtizamo unaokubalika zaidi ni kua Inakubalika na hii ni kulingana na Makisio ya Qiyas kupitia katika sababu tatu hizi ambazo ni zenye kutokana na Dharurah.'***(Sharh Sahih Muslim)*

Na Al Aalamah Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Sayyid Najmu Ad Din Shami Ibn Aabidin Al Hanafi kua: '**Ni Makruh Iliyoramishwa kufuga Mbwa kama Mnyama wa Nyumbani, ila hua inaruhusika kufuga Mbwa Kwa ajili ya Kuwindia au kwa ajili ya Ulinzi.**' *(Al Hidaya Al Aaliyah, Darru Al Muhabah)*

Ambapo amesema pia Imam Al Kasani Al Hanafi kua: **'Ama kuhusiana na Mbwa na Suali la kua kama ni Tohara ama la, basi Wanazuoni wetu wametofautiana juu yake kwani wale wanaosema kua ni Najis basi wamewaweka Kwenye Kundi moja na Nguruwe, na wale wanaosema kua ni Tohara basi wamewajumuisha na Wanyama wengine isipokua Nguruwe na huu ndio mtizamo sahih.'***(Badai Al Sanai)*

Ila kwa upande wa Madhhab ya Imam Malik basi wao wanasema kua: **'Wanyama wote wakiwa hai hua ni Tohara wakiwemo Nguruwe na Mbwa pia.'** *(Fiqh aAala Madhabib Arbaa)*

Najua kua kuna baadhi watasema kua Kufuga na kuwauza hua ni kupata Manufaa nao. Hivyo watakofikiria hivyo basi tunawarudisha katika Hadith tuliyoiangalia hapo kabla isemayo:

عن أَبِي هريرة أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: إِنَّ اللَّهَ حرم الخمر وثمنها، وحرَّم الميتة وثمنها، وحرم الخنزير وثمنه

Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameharamisha Mbwa na Bei yao, Ameharamisha Nguruwe na Bei Yao, na ameharamisha Ulevi na Bei Yake. *(Jamii Sahih, Al Awsat, Al Hawi Al Kabir)*

Ambapo hii pia hua haimaanishi kua Mbwa wanatakiwa kuuliwa, la hii haimaanishi hivyo pia kwani Dini ya Kiislam inaamrisha kua na Huruma kwa Wanyama wote isipokua wale watakaosababisha Madhara. Hivyo mbali ya kua Hadith zimeharamisha kufuga Mbwa na Wanazuoni kutofautiana juu ya Unajis wake lakini lakini hadithi zinasema kua pia hua hairuhusiki kuwauza Mbwa wala kuwaua isipokua itakapokua kuna dharurah.

Kwani amesema Imam Abu Bakr Al Shirazi Al Shafii kua: **'Kama ikiwa Mnyama atakua ni mwenye kusababisha Madhara na kutokua na Manufaa kama Mbwa mwitu, Simba, Nyoka, Nge, Panya, Kipanga, Kunguru, Mbwa Kichaa, Kunguni, Chawa n.k basi hukumu yake ni Kuuliwa ambako hua ni Sunna kwa sababu kuwaua hua ni kwenye kuondoa Madhara kwa watu.'***(Al Muhadhdhab Fi Fiqh Imam Al Shafii).*

Ambapo miongoni mwa Dharurah hizo ni kama ilivyoainishwa katika Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا مُسَدَّدٌ، حَدَّثَنَا يَزِيدُ بْنُ زُرَيْعٍ، حَدَّثَنَا مَعْمَرٌ، عَنِ الزُّهْرِيِّ، عَنْ عُرْوَةَ، عن عائشة رضي الله عنها، أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: «خمسٌ من الدَّوَابِّ كُلُّهُنَّ فَاسِقٌ، يُقْتَلنَ في الحَرَمِ: الغرابُ، وَالحِدَأَةُ، وَالعَقْرَبُ، وَالفَأْرَةُ، وَالكَلْبُ العَقُورُ».

Amesema Musaddad kau amesema Yazid Ibn ZuraiA kua amesema Muammar kua amesema Al Zuhri kuamaesema Urwat kua amesema Aisha *Radhi Allahu Anha* kua, amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua*: 'Wanyama watano ni Waovu hivyo waueni hata kama wakiwepo kwenye Ardhi takatifu mtu akiwa kwenye Ihram, nao ni Kunguru, Kipanga, Nge, Panya na Mbwa mwenye Kichaa.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

Hii ni hadith inayotaja Wanyama watano ambao ni waharibifu na wanadhuru amao ni tofauti na wanyama wengine, na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha kua wauliwe kutokana na madhara yao wanayoweza kusababisha, kiasi ya kua hata kama wakiwemo kwenye maeneo ya Ardhi takatifu na Mtu akiwa yumo kwenye Ihram basi hua inaruhusika kuwaua, na pia ndani yake wamejumuisha Wanyama wengine mithili yao.

Na pia kuna hadith isemayo kua: **'Aliulizwa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua Jee inaruhusika Kuuwa Wanyama gani Mtu akiwa kwenye Ihram?.'**

Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* akasema kua, amesema Mmoja kati ya Wake wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameamrisha kuua Mbwa Kichaa, Panya, Nge, Kunguru na Nyoka.'*(Sahih Muslim)***

Na kuna Hadith isemayo kua;

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ أَحْمَدَ بْنِ أَبِي خَلَفٍ، حَدَّثَنَا رَوْحٌ، ح وَحَدَّثَنِي إِسْحَاقُ بْنُ مَنْصُورٍ، أَخْبَرَنَا رَوْحُ بْنُ عُبَادَةَ، حَدَّثَنَا ابْنُ جُرَيْجٍ، أَخْبَرَنِي أَبُو الزُّبَيْرِ، أَنَّهُ سَمِعَ جَابِرَ بْنَ عَبْدِ اللَّهِ، يَقُولُ أَمَرَنَا رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم بِقَتْلِ الْكِلاَبِ حَتَّى إِنَّ الْمَرْأَةَ تَقْدَمُ مِنَ الْبَادِيَةِ بِكَلْبِهَا فَنَقْتُلُهُ ثُمَّ نَهَى النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم عَنْ قَتْلِهَا وَقَالَ " عَلَيْكُمْ بِالأَسْوَدِ الْبَهِيمِ ذِي النُّقْطَتَيْنِ فَإِنَّهُ شَيْطَانٌ "

Amesema Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Khalafi kua amesema Rawhu kua amesema Is-haq Ibn Mansur kua amesema Rawhu Ibn Aubadt kua amesema Abi Jurayj kua amesema Abu Zubayr kua amemsikia Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituamrisha sisi kuua Mbwa hadi ikafikia haki ya kua hata akitokea Mwanamke kutoka Jangawani na Mbwa wake basi sisi Tulikua Tukimuua Mbwa huyo, kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akatukataza na kutuambia kua : 'Mnatakiwa Muue Mbwa wenye Rangi Nyeusi tupu na Weupe chini ya Macho yao tu, kwa sababu aina hio hua ni Shaytan.'(*Sahih Muslim, Imam Ibn Majah)***

Na tunapoangalia katika *Kitab Al Mihanj* cha Shaykh Ul Islami Imam Ahu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii basi tunaona anasema kua: '**Amesema Imam Al Haramayn ambae ni mmoja kati ya Wanazuoni wetu kua: Awali *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* aliamrisha kua Mbwa wote wanatakiwa kuuliwa. Lakini baadae akatoa amri inayoibatilisha amrisho hilo, ambayo ni kua Wasiuliwe Mbwa ina yeyote isipokua Mbwa weusi Sana Na kisha ndio ikaanzishwa Hukmu ya Kutoua Mbwa aina yeyote ile iwe mweusi au mwenginewe, isipokua yule Mbwa atakaesababisha Madhara.'***(Al Minhaj)***

Na kwa upande wa Imam Ibn Qutaibah basi amefafanua kuhusiana na Mbwa Mbaya au Muovu katika Hadith inayozungumzia Mbwa weusi kwa kusema kua: '**Kwa sababu Mbwa Mweusi ndio Mbwa mkali na mbaya zaidi kuliko Mbwa wa aina nyengone zote, na pia ndio Mbwa asiekua na maana yeyote yule katika aina za Mbwa Na ni Mbwa asiefaa katika Uwindaji na Mvivi, na ameitwa Shaytan kwa sababu ni Mbwa ambae mbaya na muasi zaid kwa Ibn Adam, na ni mwenye kua na Maumbile ya Tabia kama za Simba au Mbwa mwitu anaevamia.**

Na Mbwa mweusi hua ni Mbwa ambae Mashetani na Majini hua wanapenda kumtumia kwa ajili ya kusababisha Madhara. Na kama inavyojulikana kua Shetani hua ni Jini aliesi, ama kuhusiana

na kwanini Mbwa wakawa wanauliwa katika Ardhi ya Madina Katika kipindi cha Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* basi ni kutokana na Kua Ardhi hio ilikua ndio Ardhi inayoteremshiwa Wahyi na Malaika Jibril, ambapo Malaika hua hawaingii katika Nyumba yenye Mbwa au Picha yake.' *(Ta'awil Mukhtalaf Al Hadith)*

Na tunapozungumzia Mbwa Kichaa ambae ametajwa katika Hadith kama Al Kalb Al Aqur basi pia anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: '**Wanazuoni wametofautiana Kuhusiana na maana *ya Kalb Al Aqur,* kwani kuna wasemao kua ni Mbwa wa Kawaida mwenye Kichaa, na kuna wasemao kua ni Kila Mnyama anaeshambulia hua anajulikana kua ni *Kalb Al Aqur.'*** *(Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo kwa upande wa *Mujaddid* Ad Din Imam Al Hafidh Imam Abu Fadhl Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Kuna Mitizamo tofauti kuhusiana na maana ya Kalb Al Aqur, kwanikwa upande wa Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* basi yeye amesema kua: *Kalb Al Aqur* hua ni Simba, na Mbwa anaetafuna Vibaya sana kuliko hata Atafunavyo Nyoka**. **Hivyo hii inaonesha kua Kalb Aqur hua ni Mnyama anaetafuna.**'

Kwa upande wa Zufar *Radhi Allahu Anhu* basi amesema kua Kalb Al Aqur hua ni Mbwa Mwitu Kwa upande wa Imam Malik Ibn Anas (Muanzilishi wa Madhhab ya Imam Malik) basi yeye anasema katika Al Muwatta kua: Chochote kile kinachotafuna watu na Kuwashambulia na Kuwatishia. Hivyo hata Simba, Chui, Mbwa Mwitu basi wanaweza kua ni Aqur.

Na kwa upande wa Imam Abu Hanifa basi yeye amesema kua *Kalb Al Aqur* hua ni Mbwa ambae Hukumu yake haiwezekani kujumuishwa na Hukumu ya Mnyama mwengine yeyote isipokua Mbwa Mwitu.'*(Fat-h Al Barri)*

Na akasema Imam Ibn Manzur ambae ni Muandishi wa Kamusi maarufu ya Lisan Al Arabi basi yeye anasema kua: **'Kalb Al Aqur hua ni Mnyama yeyote anaeshambulia na Kuwinda kwa kutumia Meno kwa kutafuna,Kujeruhi, Kuua na Kushambulia kwa mfano kama vile Simba, Chui, Mbwa Mwitu na Wanyama wanaofanana nao hao. Na Ameitwa Mbwa kwa sababu ya kufanana kwake na Maumbile yake.**

Ambapo kwa upande wa Imam Sufyan Ibn Uyaynah, basi amesema kua: 'Kalb Al Aqur hua ni Kila Mnyama anaeshambulia kwa kutafuna si lazima kua Mbwa, ambapo neno Aqur limetumika kuainisha Vitendo vya mashambulizi yake na hivyo hakuitwa hivyo kwa sababu ya Sifa yake bali ni kwa sababu ya kua ni Mnyama mwenye Roho.

Abu Ubayd yeye amesema kua Kila Kitu kitakachokua Kinashambulia na Kujeruhi miongoni mwa Wanyama wanaowinda hua wanaitwa *Kalb Al Aqur.'*

Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* katika Kitabu chake kitukufu katika Aya iliyozungumzia Jawarih na Mukallibin yaani Mnyama wa kufugwa wa kuwindia kua:

﴿ يَسْأَلُونَكَ مَاذَآ أُحِلَّ لَهُمْ قُلْ أُحِلَّ لَكُمُ ٱلطَّيِّبَاتُ وَمَا عَلَّمْتُمْ مِّنَ ٱلْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ تُعَلِّمُونَهُنَّ مِمَّا عَلَّمَكُمُ ٱللَّهُ فَكُلُواْ مِمَّآ أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَٱذْكُرُواْ ٱسْمَ ٱللَّهِ عَلَيْهِ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ إِنَّ ٱللَّهَ سَرِيعُ ٱلْحِسَابِ﴾

Yas-aloonaka m<u>adha</u> o<u>h</u>illa lahum qul o<u>h</u>illa lakumu al<u>t</u>tayyib<u>a</u>tu wam<u>a</u> AAallamtum mina aljaw<u>a</u>ri<u>h</u>i mukallibeena tuAAallimoonahunna mimm<u>a</u> AAallamakumu All<u>a</u>hu fakuloo mimm<u>a</u>

amsakna AAalaykum waodhkuroo isma Allahi AAalayhi waittaqoo Allaha inna Allaha sareeAAu alhisabi*(Surat Al Maidab 5:4)*

Tafsir: ***Wanakuuliza (Ewe Muhammad Salallahu Alayhi wa Salam) Jee ni kipi Kilichohalalishwa kwa ajili yao (Kukila) Sema Halali Kwenu Vilivyo vizuri na Visafi Na Mlichowafundishia Wanyama wa Kuwindia (Na wakakikamata) Waliofugwa na Kufundishwa Kuwinda Kama Alivyokufundisheni Allah Hivyo Kuleni Kile Walichokukamatieni Lakini Tajieni Jina La Allah Juu Yake Na Mcheni Allah Kwani Kwa Hakika Allah ni Mwepesi wa Kuhesabu.***

Naam..hii ni Aya inayozungumzia kuhusiana na Vilivyoruhusiwa kuliwa, ambavyo ni Vile vyote vile Vilivyokua Halali, Vitamu na Vizuri. Na kisha aya ikaendelea kudhihirisha Darja Wanyama maalum Wanaofugwa na Kufundishwa Kuwinda.

Neno *Jaraha* kwa Lugha ya Kiarabu Hua linamaanisha Jeraha, Dhuru, Faida, Kera, Tafuta, Pata au Chukua Kitu kwa ajili ya Nafsi yako. Neno *Jaraha* ndio lililotoa neno *Jawarih* ambalo humaanisha Mnyama anaewinda na Kula Nyama, Ndege anaewinda na kula Nyama na pia humaanisha Mnyama wa Kuwindia.

Ambapo kwa upande wa Bahr ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* basi yeye anasema kua: **'Neno Jawahir linajumuisha Ndani yake Mbwa na Wanyama wengineo wanaofugwa na kufundishwa Kuwinda kama Aina fulani ya Paka Wakubwa wa Jangwani, Mwewe, Kipanga na Tai**.' Ambapo huu pia ndio Mtizamo wa Imam Hasan Al Basr na Imam Mujahid.

Ambapo ingawa Wanyama wa aina hii wako tofauti kwani Ndani yake wanaingia na Ndege pia, lakini tunaona kua aya imetumia neno *Mukallib*ina ambalo ni lenye kutokana na neno Kaliba. Neno Kaliba kwa Kilugha hua linamaanisha Kubweka kwa mda mrefu.

Neno *Kaliba* ndio lililotoa neno *Kalbun* ambalo humaanisha Mbwa au Mnyama yeyote anaewinda. Na ndio maana wenye Lugha yao huwaita hata wawindao baharini kua ni *Kalb Al Bahr* yaani Samaki Aina ya Papa, na Mbwa Mwitu pia huitwa *Kalb Al Barr* yaani Muwindaji wa Ardhini.

Hivyo neno *Mukallibina* hua linamaanisha Watu wanaowafundisha Wanyama wa kuwindia namna ya Kuwinda, ambapo kulingana na Aya basi tunaona kua ili chakula kilichowindwa na Wanyama basi lazima kiwe kimekamatwa na Wanyama waliofundishwa Kuwinda na *Mukallibina* wanaotumia Njia aliyofundisha *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Na kuhusiana na Kile walichokukamatieni basi kuna Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ، حَدَّثَنَا ابْنُ فُضَيْلٍ، عَنْ بَيَانٍ، عَنِ الشَّعْبِيِّ، عَنْ عَدِيِّ، بْنِ حَاتِمٍ قَالَ " إِذَا أَرْسَلْتَ كِلاَبَكَ سَأَلْتُ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قُلْتُ إِنَّا قَوْمٌ نَصِيدُ بِهَذِهِ الْكِلاَبِ فَقَالَ الْمُعَلَّمَةَ وَذَكَرْتَ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا فَكُلْ مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكَ وَإِنْ قَتَلْنَ إِلاَّ أَنْ يَأْكُلَ الْكَلْبُ فَإِنْ أَكَلَ فَلاَ تَأْكُلْ فَإِنِّي أَخَافُ أَنْ يَكُونَ إِنَّمَا أَمْسَكَ عَلَى نَفْسِهِ وَإِنْ خَالَطَهَا كِلاَبٌ مِنْ غَيْرِهَا فَلاَ تَأْكُلْ "

'**Amesema Abu Bakr Ib Ab Shaybah kua amesema Ibn Fadhl ku amesema Bayani kua amesema Al Ashabi kua Addiy Ibn Hatim *Radhi Allahu Anhu* kua: Nilimuuliza mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kuhusiana na Mbwa wa Kwindia ambapo nae akasema:**

إِذَا أَرْسَلْتَ كِلاَبَكَ الْمُعَلَّمَةَ وَذَكَرْتَ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا فَكُلْ مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكَ وَإِنْ قَتَلْنَ

Utakapomuachia Mbwa kwa Jina la Allah (Biismi Allahi) basi Kula atakachokikamata kwa ajili yako.

Nami nikamuuliza: 'Vipi kama akimuua Mnyama aliemkamata?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema, Hamna tatizo pale itakapokua hakuna Mbwa mwengine alieshiriki katika Ukamataji huo, pale itakapokua Umemtuma Mbwa aliemtamkia Jina la Allah, na wala si Mbwa mwengine**.' *(Sahih Bukhari n Muslim)*

Ambapo katika Hadith nyengine imemalizia kwa kusema kua: **'*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Lakini kama Mbwa wakimla Mnyama huyo, basi sehemu iliyobakia Msimle kwa sababu itakua Mbwa hao wamemuwinda kwa ajili yao.'**

Hivyo Aya ya Surat Al Maidah 5:04 inayoelezea kuhusiana na Wanyama Wa Uwindaji wakiwemo Mbwa waliofunzwa namna ya Kukamata Wanaowindwa na hivyo kuthibitisha kua inaruhusika kufuga Mbwa na Wanyama wengineo wanaotumika Kuwindia na Kuruhurisika Kula Nyama ya Mnyama watakaemkamata baada ya Kusomewa Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala.*

Ambapo anasema Imam Ibn Jarir At Tabari kua: **'Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* amenukuliwa mara kadhaa akisema kua: Kama (Mbwa) Mnyama wa Kuwindia akimkamata na Kuanza Kumla Mnyama aliemuwinda, basi haitakiwi Kula sehemu ya Mnyama iliyobakia, iwe Mnyama huyo aliewinda alisomewa Bismi Allahi hapo kabla ya Kuachiwa ama la, kwani itakua Mnyama Huyo amemuwinda Mnyama Husika kwa ajili yake na wala si kama alivyofundishwa Ambapo Mtizamo huu pia ndio Mtizamo wa Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu*, Imam Ash Shabi, Imam Ataa, Imam Al Abd Rahman Sudi na wengineo.**

Na Adiyy Ibn Hatim *Radhi Allahu Anhu* amenukuu Hadith yenye Maneno kama aliyoyasema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* katika Fatwa yake. Lakini hata hivyo Sharti hili hua halihitajiki Kusimamiwa kwa upande wa pale inapokua Mnyama Muwindaji ni Ndege.

Kwani kwa upande wa Ndege basi kinachotakiwa ni kua Ndege huyo aliewinda arudi kwa Mmiliki wake yaani Muwindaji baada ya kukikamata kile alichokiwinda, na aiifanya hivyo basi Ndege husika huingia katika kua na Sifa ya Mnyama wa Kuwindia aliefunzwa kuwindia, na hivyo kile walichokiwinda hua inaruhusika kukila hata kama Wataanza kukila wao.

Ambapo kwa upande wa Ali Ibn Abi Talib *Radhi Allahu Anhu,* Imam Said Ibn Jubayr, Imam Ikrima na wengineo basi wao wanasema kua Hakuna Tofauti baina ya Wanyama na Ndege Wa Kuwindia, hivyo kama wakianza kukika kile walichokiwinda basi hua hairuhusiki kwa Muislam kukila kitu hicho.' *(Tafsir Imam At Tabari)*

Na kama tulivyoona hapo kabla kua pia kuna Hadith iliyomo katika Sunnan Abu Daud ambayo inasema kua: '**Kama Mkimuchia Mbwa kwa Jina la Allah kuwinda, basi kuleni kile alichokiwinda hata kama itakua wameshaanza kukila.'** *(Sunnan Abu Daud, Sunan An Nasai)*

Ambapo tunapoziangalia Hadith hizi zilizonukuliwa na Maimamu Wawili hawa basi tunaona kua ni Hadith zinazoaminika kua ni Sahih, na haya yanathibitishwa na Mtizamo wa Salman Al Farisy, Abu Hurayrah, Sad Ibn Abi Waqqas, Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhum*, Imam Qatadah Ibn Diama Al Sadusi ambao wao wanakubaliana na Hukumu ya Hadith hii kua Inaruhusika Kula Mnyama husika aliewindwa hata kama itakua ameshaliwa na Mnyama wa Kuwindia kama alivyosema Mujaddid Ad Din Imam Fakhr Ad Din Al Razi katika *Mafatih Al Ghayb.*

Imam Fakhr Ad Din Al Razi anaendelea kusema kua : **'Imam Al Juwayni Al Shafii na wengineo wamezisuluhisha Hadith mbili hizi zinazopingana kwa kusema kua: 'Hivyo kama ikiwa Mnyama wa Kuwindia ameanza kumla Mnyama aliemuwinda mara tu baada ya Kumkamata, basi ni Bora kutokula sehemu yeyote ya Mnyama aliewindwa Lakini Kama ikiwa Mmiliki wa Mnyama Muwindaji amechelewa kuwasili kwenye Mnyama aliekamatwa na Mnyama aliewinda, na alipofika akakuta kua Wanyama wawindaji wameshaanza kumla Mnyama aliewindwa, basi hapa hua inaruhusika kula sehemu ya Mnyama aliewindwa.**

Na kuhusiana na Kutajia Jina la *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa mnyama wa Kuwinda unapomuachia, basi Wanazuoni wametofautiana juu yake kwani kuna Wanaosema kua Kutajia Jina la Allah hua ni Lazima, na kuna wanaosema kua Sio lazima hivyo kama ikiwa umesahau basi hamna tatizo.' *(Mafatih Al Ghayb)*

Na pia anasema Imam Muslim Ibn Hajjaj kua:

حَدَّثَنَا إِسْحَاقُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ الْحَنْظَلِيُّ، أَخْبَرَنَا جَرِيرٌ، عَنْ مَنْصُورٍ، عَنْ إِبْرَاهِيمَ، عَنْ هَمَّامِ بْنِ الْحَارِثِ، عَنْ عَدِيِّ بْنِ حَاتِمٍ، قَالَ قُلْتُ يَا رَسُولَ اللَّهِ إِنِّي أُرْسِلُ الْكِلاَبَ الْمُعَلَّمَةَ فَيُمْسِكْنَ عَلَىَّ وَأَذْكُرُ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ فَقَالَ " إِذَا أَرْسَلْتَ كَلْبَكَ الْمُعَلَّمَ وَذَكَرْتَ اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ فَكُلْ " . قُلْتُ وَإِنْ قَتَلْنَ قَالَ " وَإِنْ قَتَلْنَ مَا لَمْ يَشْرَكْهَا كَلْبٌ لَيْسَ مَعَهَا " . قُلْتُ لَهُ فَإِنِّي أَرْمِي بِالْمِعْرَاضِ الصَّيْدَ فَأُصِيبُ فَقَالَ " إِذَا رَمَيْتَ بِالْمِعْرَاضِ فَخَزَقَ فَكُلْهُ وَإِنْ أَصَابَهُ بِعَرْضِهِ فَلاَ تَأْكُلْهُ ".

Amesema Is-haq Ibn Ibraahim Al Handhali kua amesema Ibrahim Jariri kua amesema Mansuri kua amesema Ibrahim kua amesema Hammam Ibn Harith kuaamesema A Kwani anasema Addiy Ibn Hatim *Radhi Allahu Anhu* kua: Nilimwambia Mimi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Ya Rasul Allah, Nilimwachia Mbwa wangu mimi kuniwindia na Nikatamka Jina la Allah juu yake.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Utakapomtauarisha Mbwa wako kisha ukatamka Jina la Allah na Kumuachia, basi kula Alichokamata.'**

Nami nikasema: '*Ya Rasul Allah!* Hata kama Mbwa wangu hao itakua Wamemuua Mbwa huyo?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: 'Naam..Hata kama watamuua, lakini kwa sharti iwe ni Mbwa wako hao waliofanya hivyo na isiwe Mbwa mwengine amechangia katika Kukamata mnyama anaewindwa.'**

Nami nikasema: 'Na kama Nimemrusha Mirad (Ndege) Kwa ajili ya Kuwindia?'

Rasul Allah Salallahu Alayhu wa Salam **akasema: 'Utakapomrusha Mirad na kisha Akampasua Mnyama aliemuwinda, basi Mle, lakini kama akimpiga Aliemuwinda na Akaanguka na kufa kaa muanguko huo basi Usimle.'***(Sahih Muslim)*

Na kaika hadith nyengine imesemwa kua;

حَدَّثَنَا هَنَّادُ بْنُ السَّرِيِّ، حَدَّثَنَا ابْنُ الْمُبَارَكِ، عَنْ حَيْوَةَ بْنِ شُرَيْحٍ، قَالَ سَمِعْتُ رَبِيعَةَ بْنَ يَزِيدَ الدِّمَشْقِيَّ، يَقُولُ أَخْبَرَنِي أَبُو إِدْرِيسَ، عَائِذُ اللَّهِ قَالَ سَمِعْتُ أَبَا ثَعْلَبَةَ الْخُشَنِيَّ، يَقُولُ أَتَيْتُ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَقُلْتُ يَا رَسُولَ اللَّهِ إِنَّا بِأَرْضِ قَوْمٍ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ نَأْكُلُ فِي آنِيَتِهِمْ وَأَرْضِ صَيْدٍ أَصِيدُ بِقَوْسِي وَأَصِيدُ بِكَلْبِيَ الْمُعَلَّمِ أَوْ بِكَلْبِيَ الَّذِي لَيْسَ بِمُعَلَّمٍ فَأَخْبِرْنِي مَا الَّذِي يَحِلُّ لَنَا مِنْ ذَلِكَ قَالَ أَمَّا مَا ذَكَرْتَ أَنَّكُمْ بِأَرْضِ قَوْمٍ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ تَأْكُلُونَ فِي آنِيَتِهِمْ فَإِنْ وَجَدْتُمْ غَيْرَ آنِيَتِهِمْ فَلاَ تَأْكُلُوا فِيهَا وَإِنْ لَمْ تَجِدُوا فَاغْسِلُوهَا ثُمَّ كُلُوا فِيهَا وَأَمَّا مَا ذَكَرْتَ أَنَّكَ بِأَرْضِ صَيْدٍ فَمَا أَصَبْتَ بِقَوْسِكَ فَاذْكُرِ اسْمَ اللَّهِ ثُمَّ كُلْ وَمَا أَصَبْتَ بِكَلْبِكَ الْمُعَلَّمِ فَاذْكُرِ اسْمَ اللَّهِ ثُمَّ كُلْ وَمَا أَصَبْتَ بِكَلْبِكَ الَّذِي لَيْسَ بِمُعَلَّمٍ فَأَدْرَكْتَ ذَكَاتَهُ فَكُلْ "

Amesema Hanad Ibn Sariu kua amesema Ibn Mubarraka kua amesema Haywat Ibn Shuyhmrayh kua amesema Rabia Ibn Yazid Ad Dimashq kua amesema Abu Idrisa kua amesema Abu Thalabah Al Khushani *Radhi Allahu Anhu* kua: *Ya Rasul Allah,* hakika sisi tunaishi katika Ardhi yenye Watu wa Ahl Al Kitab, hivyo tunakula katika Vyombo vyao, na Tunaishi katika maeneo ambayo ni maarufu kwa Uwindaji.

Hivyo hua nnawinda kwa Kutumia Upinde wangu na nnawinda kwa kutumia Mbwa ambae Nimemfundisha Kuwinda, na baadhi ya wakati na mbwa ambae hakufundishwa Kuwinda, Hivyo niambie kipi ni Halali katika haya.

Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam **akasema: Ama kuhusiana na Watu wa *Ahl Al Kitab* unaoishi nao na kula katika Vyombo vyao, basi kama utapata vyombo vyengine zaidi ya hivyo usitumie vyao, Lakini kama ukikosa basi kosha hivyo vyao na kisha Kulia.**

Ama kuhusiana na Kuishi kwako katika ardhi Maarufu kwa Uwindaji Basi Unawinda kwa kutumia Upinde, kitamkie Jina la Allah katika Wakati unauachia Upinde na kisha kula ulichokiwinda.

Na kile unachokiwinda kwa Kutumia Mbwa basi Tamkia Jina la Allah pale unapomuachia Mbwa wako na kisha kula alichokikamata.

Na kile utakachokikamata kutokana na Mbwa wako ambae hujamfundisha Kuwinda na kama itakikuta kikiwa hai basi kichinje kulingana na Sharia na kisha Kula.'*(Sahih Muslim)*

Ambapo amesema Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii kua: **‘Mbwa aliefundishwa Kuwindwa hua ni yule anaewinda kutokana na kufuata amrisho la Muwindaji.**

Hivyo hua hamli Mnyama aliemuwinda, na kama atafanya kama ulivyomfundisha, basi atakua ni Mbwa aliefundishwa kuwinda, na hivyo akimkamata Mnyama aliemuwinda basi hatomla, na Hivyo Muwindaji yaani Mmiliki wake Mbwa huyo ataruhusika kumla Mnyama huyo aliewindwa, na hivyo Mbwa akimla Mnyama aliemuwinda, basi Mbwa huyo atakua hakufundishwa Kuwinda*(Kitab Al Umm)*

Am akuhusiana na Kanuni za Mbwa,Mnyama au Ndege Muwindaji ili kikubalike Uhalali wake kile alichokiwinda basi hutakiwa kutimiza masharti yafuatayo:

1-Mnyama/Ndege Husika awe ni Aliefundishwa Kuwinda, na hivyo awe halikile anachokikamata, bali anakikamata kwa aili ya Muwindaji/Mmiliki, anatii Maamrisho ya Mmiliki/Muwindaji hivyo kama akiamrishwa anatii na akikatazwa anaacha alichokatazwa, anapoitwa anakuja.

2-Anatakiwa aachiwe na Muwindaji wake kwa ajili ya Kuwinda Mnyama husika, hivyo kama akikimbilia mwenyewe basi aliewindwa hua haram kumla.

3-Wasikile hapo hapo kile walichokikamata.

4-Wawe wametamkiwa Bismi Allahi wakati wanapoachiwa.

5-Mnyama anatakewindwa kama akifa kutokana na Majeraha ya Kuwindwa, basi anaruhusika kuliwa lakini, Kama akifa katika Harakati za Kukimbia, akajigonga labda au akaanguka basi hua haram kuliwa na Muwindaji ni Ndege basi akimuangusha Mnyama aliemuwinda na hivyo Mnyama akafa kutokana na Muangusho huo, basi Mnyama husika hua Haram kumla.

6-Mnyama Akikutwa Hai basi achinjwe Kislam.

7-Mnyama anaewindwa awe ni wa Mwituni ambae ni Halali kuliwa, hivyo kama ikiwa ni Mnyama wa Kufuga au tayari ameshakamatwa na kisha akauliwa na Mnyama wa Kuwindia basi Mnyama husika hua haram kumla.

8-Muwindaji asiwe katika Hali ya Ihram ya Ibada ya Hija au Umra, kwani imeharamishiwa Kuwinda katika wakati Mtu akiwa katika Ihram.

﴿أُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ ٱلْبَحْرِ وَطَعَامُهُ مَتَاعاً لَّكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ وَحُرِّمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ ٱلْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرُماً وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ ٱلَّذِيۤ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ﴾

Ohilla lakum saydu albahri wataAAamuhu mataAAan lakum walilssayyarati wahurrima AAalaykum saydu albarri ma dumtum huruman waittaqoo Allaha alladhee ilayhi tuhsharoona*(Surat Al Maidah 5:96)*

Tafsir: ***Halali kwenu nyinyi kuwinda Wanyama wa Majini na kuwtumia kwa ajili ya chakula, kwa manufaa yenu na kwa wale walio safarini, lakini mmeharamishiwa kuwinda pale mnaokua kaika hai ya Ihram(ya Hija au ya Umra) na muogopeni Allah ambae kwake yeye mtarudishwa na kukusanywa Pamoja.***

Ambapo anasema Muwaffaq Ad Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: **‘Wanyama wote wanaoweza Kufugwa kufundishwa na Kuwinda kama Chui au Ndege wanaokula Nyama hua wanaingizwa kwenye Hukumu sawia na Hukumu ya Mbwa wa Kuwindia,katika Kuruhusika Kuwatumia katika Uwindaji, hivyo ndivyo alivyosema Imam Abu Hanifa, Imam Malik na Imam Al Shafii.’***(Al Mughni)*

Na anasema Imam Abu Abd Allah Muhammad Ibn Ahmad Ibn Abi Bakr Al Qurtubi Al Maliki kua: ‘**Ama kuhusiana na kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua "Kama Ukimtuma" ambayo inamaanisha kua Mtumaji anatakiwa kua ni Muwindaji na kwa ajili yake kwa sababu Af'ala hua ni kitendo cha Mfanyaji kama ilivyo Akhraja na Akram**. **Hivyo Kitendo hiki hua ni cha Kiakili na chenye Makusudio yamayokubalika**. **Na juu yake kuna mambo mawili**

1-Muwindaji lazima awe ni mwenye Makusudio ya Kumchinja Mnyama anaemuwinda na hivyo anatakiwa afanye jambo hilo kua ni lenye Kuruhusika katika kumtuma Mnyama wake wa kuwindia, na juu ya hili kuna makubaliano juu yake.

2-Mbwa husika anatakiwa kua aachiwe na Muwindaji, yaani Muwindaji awe na Hatamu ya Mbwa wake na kisha aiachie huku akimuashiria Mnyama anaewindwa ili afukuziwe. Au kama ni anaetumika katika Kuwinda ni Ndege basi Ndege huyo anatakiwa awe ametulia kabla ya Kumkimbilia Mnyama amuwindae, na hatomfukuzia hadi pale atakapoashiriwa na Muwindaji, jambo ambalo ni sawa na mtu mwenye hatamu zake na kisha akaziachia.

Hivyo kama Mnyama akitoka na kufukuzia mwenyewe bila kuashiriaa basi hua haruhusiki kumtumia katika Uwindaji, na akichokikamata hua hakiruhusiki kukila, kwa sababu Mnyama husika hua amejiwindia kwa ajili yake Na hivyo Maneno ya yasemayo kua "Kama Mkiwaachia Wanyama wenu" hua Hayajafanya kazi na hakuna kutokukubaliana juu ya Hili kutokana na ninavyojua.’(*Al Mufhim)*

Na Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi akasema kua: **‘Ama kuhusiana na maneno ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* yasemayo kua: Kama Mbwa uliemtuma akimkamata Mnyama anaewindwa na ukamkuta nae akiwa hai, basi Mchinje.**

Hivyo hii inamaanisha kua Mnyama husika anaewindwa akipatikana basi na Achinjwe Hivyo hatokubalika kuliwa hadi Achinjwe, na juu ya hili kuna makubaliano pia. **Na kama akimfikia Mnyama huyo na kumkuta kua ameshakufa, kwa kuchanwa Koromeo lake au Tumbo lake,au kiungo cha ndani ya mwili wake kimetoka nje, basi hua inaruhusika bila kumchinja, na juu ya hili kuna makubaliano pia.**

Ambapo As-hab wetu wamesema kua inapendekezwa Kupitisha Kisu kwenye Koromeo lake ili kumrahishia kumalizika kwa kiuhai.’(*Sharh Sahih Muslim)*

Kwa maana hio basi kama ikiwa Mnyama Muwindaji ni Mnyama asiefugwa au aaiefundishwa kuwinda kama Simba, Chui, Mbwa, Mbwa Mwitu, n.k akashamshambulia Mnyama anaeliwa na akafa, basi Mnyama huyo hua haruhusiki Kuliwa, na juu ya hili kuna makubaliano ya Wanazuoni.

Lakini kwa upande mwengine basi anasema Imam Al Qurtubi kua: **‘Amesema Imam Sufyan Ibn Uyaynah kua amesema Sharik kua amesema Jariri kua amesema Ar Rakiin Ibn Rabii kua amesema Abu Talha kua amesema Mimi nilimuuliza Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kuhusiana na Mbwa mwitu ambae amemshambulia Kondoo na kumrarua Tumbo lake, hadi Utumbo wake ukatoka Nje.**

Na hivyo mimi nikatokea na Kumkuta katika Hali hio akiwa anahema na nikamchinja. **Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* akasema: Mle, lakini usile katika Upande aliochanwa Tumbo lake.'*(*Jamii Al Ahkami Imam Al Qurtubi)*

Na anasema Imam Ibn Abd Al Barr Al Maliki Al Andalusi kua: '**Imam Is-haq Ibn Rahawayh amesema kua: 'Ama kuhusiana na Kondoo alieshambuliwa na Mbwa Mwitu na kuraruliwa Tumbo lake, na Utumbo ukatoka nje na hivyo kujulikana wazi kua hatoweza kuishi basi Sunnah yake juu yake ni kama alivyosema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu.***

Na hii ni kwa sababu hata kama Utumbo wake umetoka Nje lakini bado yuhai na sehemu ya Kumchinjia ni salama, basi hapa Suali hua haliwi kama Kondoo ataishi ama la bali hua yuhai kumchinja ama la.

Ama kuhusiana na Mnyama anaeumwa na huenda akafa basi anatakiwa achinjwe kama hajafa Na yeyote anaesema vyenginevyo basi hua ameenda kinyume na Sunnah za wengi Miongoni mwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum* na Wanazuoni.'*(Al Tah-mid)***

Naam baada ya kuangalia vithibitisho vya Aya na Hadith kuhusiana na kuruhusika kufuga Mbwa Mnyama ambae kila kitu chake Ni Najis kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii, ila kuruhusika huko hua ni kwa sharti la kua ni Lazima Mbwa husika awe ni kwa ajili ya Kuwindia au kwa Ajili ya Ulinzi kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* Kua: Mtu yeyotw atakaefuga Mbaa ambae hatumiki kwa ajili ya Kuwindia wala kulindia Mifugo au Shamba basi atapoteza *Qirat* Mbili ya Malipo mema yake katika Kila siku yake.

Na hivyo Imam Al Khatib Al Shirbini Al Shafii akasema kua : **'Inaruhusika Kufuga Mbwa kwa ajili ya Kuwindia au Kulindia Mifugo ay Shambani na pia kufuga Mbwa mdogo hadi awe Mkubwa kwa ajili ya Malengo hayo.'***(Al Mughni Al Muhtaj)*

Hivyo tunamuangalia Al Hafidh Al Kabir Al Mutqin Al Muhariri Imam Zayn Ad Din Abd Rahman Al Iraqi Al Shafii ambae anatuambia kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii juu ya Kufuga Mbwa kua: '**Kama ikiwa Mtu atafuga Mbwa ambae hajafunzwa Kuwinda, kwa malengo ya kua atamfundisha Kuwinda, basi hua inaruhusika kama Mbwa huyo ni Mkubwa.**

Na kama ni bado mdogo na akaamua Kumfuga na Kumfundisha kuwinda basi Wanazuoni wetu wana Mitizamo miwili Juu yake, ambapo Mtizamo wa Kwanza ambao ndio sahih basi hua inaruhusika pia, kama zilivyosema Hadith kuhusiana na Kuwind kwa kutumia Mbwa, na kwa sababu tunaemzungumzia hapa ni Mbwa wa Kuwindia.

Hivyo kama ingekua hairuhusiki basi isingewezekana kuwafundisha Mbwa, kwani haiwezekani Kuwafundisha Mbwa bila ya kuwafuga.'*(Tarh Al Tadhrib)*
Ambapo kwa Upande wa *Al Faqih Al Aallamah* Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Al Shafii amesema kua Hairuhusiki kufuga Mbwa isipokua kwa Kuwindia, Kulindia Mifugo, Shamba na mambo ya mithili ya hayo. Na hivyo Kama alivyosema Al Shafii, hairuhusiki kufuga Mbwa isipokua pale Mbwa huyo atakapokua ana Manufaa, na hapo ndio itaruhusika Kumfuga.**

Ama kwa upande wa Imam Abu Hanifa basi yeye amesema kua: Inaruhusika Kufuga Mbwa kwa vyovyote vile hata kama ikiwa hana manufaa. Na hii ni kutokana na Ukweli wa kua Kila Mnyama

ambae Anaruhusika Kufuga hua na Manufaa, hivyo hua inaruhusika kufuga aina zote za Wanyama wanaofugika hata kama watakua hawana manufaa.'

Imam Al Mawardi anaendelea kusema kua: **'Lakini uthibitisho wetu sisi (Wafuasi wa Madhhab ya Imam Al Shafii) ni kutokana na Hadith ya Malik kutoka kwa Nafii kutoka kwa Ibn Umar kutoka kwa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambae amesema kua: Yeyote atakaefuga Mbwa asiekua wa Kuwindia wala Kulindia basi atapunguziwa Qirat mbili kutoka katika malipo ya Amali Njema zake katika kila siku.**

Na hivyo kutokana na hii basi inanesha kua Mbwa hua kuna aina mbili, kuna Mbwa wenye Manufaa na wasiokua na Manufaa. Ambapo Kufuga Mbwa asiekua na Manufaa kumeharamishwa na hii ni kutokana na Hadith tuliyoiangalia ya Malaika Jibril alipomwambia *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Malaika hawaingii kwenye Nyumba yenye Mbwa au yenye Picha.

Na kama Mbwa akiwa na Kichaa ndio Kabisa, inabidi auliwe kwa sababu hua ana madhara na hii ni kutokana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* aliposema kua Mbwa ni Waovu hivyo waueni Weusi na weupe miongoni mwao.

Na pia kuna Hadith isemayo kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipohamia Madina aliamrisha Kuuliwa kwa Mbwa, ambapo kuna Mtu aitwae Abu Muhammad ambae alikua akiwazunguka na Mshale na kuwaua.

Lakini kwa wale wanyama wasiokua na Madhara na wasiokua hatari basi hua hairuhusiki Kuwaua na hii ni kutokana na hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* isemayo kua: Kwa kila Kiumbe kilichokua Hai basi hua kina Thawabu juu yake.'*(Al Hawi Al Kabir)*

Al Faqih Al Aallamah Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii anaendelea kutuambia kua: '**Ama kuhusiana na Mbwa wanaoruhusika Kufugwa kutokana na Manufaa yao kulingana na Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ambao ni wa Kuwindia na wa Ulinzi wa Mifugo na Shambani Ambapo kuhusiana na Mbwa wa Kuwindia ameruhusiwa kufugwa kwa sababu Kuna Wanyama ambao wanawindwa na Wanyama wenzao kwa mfano kama Sungura, hivyo hua kuna haja ya Kumuliki Mbwa wa Kuwindia.**

Am kuhusiana na Mbwa Mlinzi wa Shambani kwa wenye Mashamba basi ni kwa sababu ya Ulinzi wa Mazao hususan katika wakati wa Usiku kutokana na Ukubwa wa hisia zao na kutokua na usingizi mzito, hivyo hakuna anaeweza kuchukua nafasi ya Mbwa katika hilo na ndio maana Na ndio maana ikaruhusika kwao kuwafuga.

Ama kuhusiana na Mbwa wa Ulinzi wa Mifugo, basi ndi Mbwa ndio wanaowasimamia Kondoo wanapokua wanakula Majani, na hivyo kuwalinda dhidi ya Wanyama Wakubwa na Wadogo wenye Madhara nao, hivyo Wafugaji huwahitajia Mbwa na hivyo ikaruhusika kwao kuwafuga, na pia imeruhusika kwa wenye aina nyengine za Mifugo.

Ama kuhusiana na Mabedui wanaoishi kwenye Mahema Majangwani Basi imeruhusika kwao wao Kufuga Mbwa kwa ajili ya Ulinzi dhidi ya Wavamizi na Wanyama wenye Madhara, kwani kutokana na Mbweko wa Mbwa wanapppna Mtu wasiemjua huwataarifu Wenyeji juu ya ya Ugeni huo na hivyo Kuamka na Kuangalia Usalama wa Makazi yao.

Na hii pia hua si kwa Mabedui wenye Mahema au Hema moja moja tu Jangwani au Nyumba nje ya Mji bali inaruhusika hata kwenye Ngome, na kwenye Misafara ya Safari tofauti Kwani imenukuliwa kua Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* alionekana akienda kwenye Ibada ya Hija akiwa amefuatana na Mbwa.

Hivyo akaulizwa: "Unaenda Katika Ibada ya Hija na Mbwa?" Ambapo nae akasema: "Naam, Huyu Ni Mlinzi wa Nguo zetu"

Ila kuhusiana na Kufuga Mbwa wa Ulinzi wa Makazi Kwenye Miji basi katika Madhhab yetu ya Imam Al Shafii kuna Mitizamo Miwili juu yake.

Na Mtizamo wa kwanza ni wa Imam Abu Is-haq ambae amesema kua Inaruhusika kuwafuga Kwa sababu ya Umakini wao na kuwabwekea wale wasiowajua, hivyo hua inaruhusika.

Na mtizamo wa pili ni kua hairuhuaiki kuwafuga Mbwa Mijini, kwa sababu Mijini kuna watu wengi ambao wanaweza kuwazoea Mbwa kiasi ya kua Mtu anaweza kumhadaa Mbwa kwa kumpa chakula hadi akamzoea, na kisha akaja Usiku na Kuiba bila kubwekewa.

Jambo ambalo ni tofauti na Mbwa anaelinda Shamba na Mifugo ambae hulinda dhidi ya Madhara ya Wanyama Pori Hivyo kuna utofauti baina ya aina hizi za Mbwa hawa.

Ama kuhusiana na Kufuga Mbwa wadogo kwa ajili ya kuwafundisha Kuwinda, Kulinda Mazao au Mifugo, basi hua kuna Mitizamo miwili juu yake.

Ambapo Mtizamo wa kwanza ni kua haikubaliki na hii ni kwa sababu Mbwa hao kwa wakati huo hua hawana Manufaa.

Na mtizamo wa pili ni kua Inaruhusika kuwafuga kwa ajili ya Kuwafindisha, ambako hua kuna manufaa, na kwa sababu haitowezekana kwao Kuwinda bila Kufundishwa hivyo kama ikiwa ni haramu kuwafundisha Kuwinda basi na Kuwindia pia itakua haramu.

Ama kuhusiana na Mbwa wenye Kujua Kuwinda na Kulinda lakini wakawa wanafugwa na Asiewatumia kwa Manufaa hayo,basi kuna Mitizamo miwili juu yake na Mtizamo wa kwanza ni Kua inakubalika kutokana na Manufaa yao ya Kimaumbile. Na mtizamo wa Pili ni kua Haifai kwa sababu hawamnufaishi anaewafuga.'*(Al Hawi Al Kabir Fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Hivyo Al Faqih Al Aallamah Imam Ali Ibn Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii anaendelea kutuambia kua: '**Hukmu ya Suali la Kufuga Mbwa hua ni Kua Hairuhusiki, isipokua pale itakapokua Kuna Manufaa kutokana nao,hivyo kama ikiwa Mbwa husika ana Manufaa basi hua Inaruhusika kumfuga.'***(Al Hawi Al Kabir Fii Fiqh Madhhab Al Shafii)*

Na kama tulivyoona hapo kabla kulingana na Vithibitiho vya Hadith kama alivyosema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam kua* Manufaa ya Mbwa hua ni Kuwindia na Kulindia. Na bila ya shaka haya ndio yaliyokua Matumizi ya Mnyama Mbwa katika mazingira ya wakati huo, lakini hata hivyo tunapoangalia katika hali ya Mazingira ya leo basi tunaona kua Mbwa hua wanatumika pia kwa matumizi mengineyo yenye kunufaisha kwa Mfano: '**Kusaidia Kunusa Mihadharati, Mabomu, katika maeneo ya Mipaka ya Kuingilia na kutokea ardhi za Nchi tofauti kama Uwanja wa Ndege, Bandarini n.k Hutumika katika Kunusa Harufu za Watu katika Kusaka Wahalifu, katika Uokozi wa Maisha ya Watu katika maeneo yaliyofikwa na Maafa kama ya Mafuriko, Maporomoko ya Ardhi, Mitetemeko ya Ardhi n.k.'**

Mbwa pia hutumiwa katika Kuwasaidia Watu wasioona katika safari zao za kila siku za hapa na pale n.k.

Na bila ya shaka haya yote hua ni Manufaa ya Mbwa wale ambao Wamefugwa na Kufundishwa namna ya Kuwasaidia Ibn Adam kulingana na Mafunzo ya Mbwa husika kama vile inavyokua wanafunzwa katika Undaji.

Na kama tunavyojua kua Moja kati ya Kanuni za Sharia za Allah Subhanah wa Ta'ala Juu ya Viumbe wake ambao ni Ibn Adam basi ni kua Kuzuia Madhara na kuwaondolea Ugumu wa Mambo katika Maisha yao ya Kila siku.

Na hakuna hata mmoja miongoni mwetu akataekataa kua Matumizi haya ya Mbwa hua ni yenye Kuleta Manufaa kwa Ibn Adam na pia kuwarahisishia Ibn Adam katika Ugumu wa Mambo ambao uko nje ya uwezo wao, na hivyo katika Hali kama hizi basi pia hua inaruhusika Kufuga Mbwa, kwa ajili ya Utekelezaji na urahisishaji wa Jambo husika lenye Ugumu au Uzito kulingana na Mafunzo aliyopewa Mbwa husika.

Na hivyo kwa watu wenye kua katika Mazingira kama haya ya kufuga Mbwa Basi mbali ya kua kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Mbwa ni Najis Mughallazah na hivyo ukigusana na Kitu chochote chenye Umaji maji kutoka kwake basi hukubidi Kuitoharisha mara 7, mara moja kwa mchanga sehemu ya Kitu chako kilichogusana nae.

Lakini kwa Upande wa hali ya Mazingira kama haya ya Dharurah basi hua inaruhusika Kugusana nae kwa sababu hii hua tayari ni hali ambayo kifiqh hua inajulikana kama *Ummum Al Balwa*. Ambapo hapo kabla tulisema kua Ummum Al Balwa hua Ni Kitu kuingizwa katika Hali ya Kudhaurilika Hukmu yake kutokana na kutokuwepo uwezekano wa Kukiepuka.

Hivyo basi Hukmu ya Mbwa katika hali za Mazingira kama haya ya Kuwasaidia Vipofu katika harakati zao za kila siku za Kimaisha, ambapo hua Ngumu bila kua nao, Au Kuwatafuta Waliopotea kwenye Mitetemeko ya Ardhi kua Vigumu kuwapata bila kua na Mbwa wa Kujusa harufu zak, au Kuzuia Mabomu au Mihadharati ambayo ni Vigumu kuijua bila Mbwa kunusa n.k hua ni sawa na Hukmu ya Mbwa wa Kuwindia ambae mbali ya kua Mate yake ni Najis lakini Kile akikamatacho baada ya kukiwinda hua inaruhusika Kukila.

Hivyo kulingana na Shariah za Kiislam Hua Hairuhusiki Kufuga Mbwa isipokua kwa ajili ya Jambo maalum lenye kuruhusika Kutokana na Manufaa yatakayopatikana kutokana nabMbqa huyo, kama tulivyoona kwenye Mifano hapo kabla, Na hii ni kwa sababu ya kua kama alivyosema **Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaefuga Mbwa asiekua wa Kuwindia, kwa Ajili ya Ulinzi wa Wanyama na Shambani basi atafutiwa Qirat mbili za Malipo ya Mema yake ya Kila Siku-*Sahih*** *Muslim)*

Hivyo haina haja Kuiga Mambo ya Kimagharibi, na kisha kujifutia Amali njema zenye Ukubwa wa Qirat mbili ambao ni sawa na Malipo ya kutoa Milima Uhud miwili ya Dhahabu kwa ajili ya Sadaka ambazo badala ya Kujikusanyia basi Unajifutia kutoka katika Thawabu zako. Lakini Mbwa anapokua katika hali ya Kufugwa kutokana na Manufaa husika basi hua anahesabika sawa na Mnyama mwengine wa Kufuga ambae Nyama yake hua hailiwi na pia hua anahesabika kua ni Najis.

Kwani anasema Imam Jamal Ad Din Abu Muhammad Abd Rahim Ibn Al Hasan Al Umawi Al Qurashi Al Isnawi Al Shafii Al Masri kua: '**Ruhusa ya Kufuga Mbwa kwa ajili ya Kuwindia kutokana na**

Kufundishwa kuwinda na kutumiwa na Wanaowinda na Mbwa hua Inaruhusika Lakini Kufuga kwa ajili ya Wasiowindia hua Haikubaliki.' *(Al Muhimat Fi Sharh Al Rawda wa Al Rafii)*

Ambacho hiki ni kitabu kinavichofafanua vitabu va Maimamu wawili wa juu kabisa Fatwa wa Fiqh Madhhab ya Imam Al Shafii ambavyo ni *Rawdah At Talibin* cha Imam An Nawawi na *Fat-h Al Aziz* cha Imam Al Rafii.

Na hivyo Imam Al Isnawi kudhihirisha ndani yake juu ya Mtizamo huu kua ndio Mtizamo wa Imam An Nawawi na pia Imam Al Rafii, na hivyo kua na Makubaliano kua Haikubaliki kufuga Mbwa bila ya Kua na Manufaa nae, na hivyo kwa wale wanaoruhusika Kufuga kutokana na Manufaa nao kama Wawindaji, Walinzi,Majeshi, Wafugaji, Wakulima, Vipofu n.k.

Hua Wanaruhusika lakini Unajis wake hua hautoweki, kwani hivyo Mfugaji hua anatakiwa kua Makini nao kwani vyenginevyo basi itambidi kila kitu chake akikoshe Mara 7, kitakapoguswa na Mate, Manyoya na maji maji ya aina zote yatakayogusana na Mbwa huyo. Kwa sababu hata huyo Mbwa Wa Kuwindia, Kulindia na Kufugia hua hatakiwi Kugusana nae ovyo ovyo.

Na hivyo Mtu anaeruhusika Kumtumia Mbwa kutokana na sababu Maalum inayokubalika Kisharia, hua hatakiwi Kusalia Nguo hizo hizo alizogusana na Mbwa wake huyo kwani hua zina Najis.

Bali Hua anatakiwa Kusalia na Kufanyia Ibada Nguo Nyengine zilizokua Tohara, ambazo ni tofauti na alizotumia wakati alipogusana na Mbwa wake Yaani hii hua inakua sawa sawa na Mithili ya Mtu anaeuza Nyama, hua haiwezekani kutokua na Damu katika Nguo au Mwili wake.

Kwani hata tunapoangalia kuhusiana na sehemu ya Nyama ya Mnyama alietafunwa na Mbwa wa Kuwindia katika wakati wa Kumkamata basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii wametofautiana juu yake kama anavyosema Sultan Al Ulamaa Imam Izz Ad Din Ibn Abd Salam Al Shafii kua: '**Kuna Mitizamo mwili kwa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Al Shafii Juu ya eneo la Jeraha alilojeruhiwa Mnyama aliewindwa na Mbwa baada ya kukamatwa kwake, kwani Mtizamo wa kwanza unasema kua: Linahesabiwa kua ni *Ummu Al Balwa* (Linadharaulika)**. **Na mtizamo wa pili unasema kua Inabidi sehemu ya Jeraha husika ikoshwe mara 7 ambapo mara moja kwa Mchanga.'***(Al Ghaya Fi Al Ihtisar Al Nihaya)*. Na hivyo ndivyo pia alivyosema Imam Al Rafii Al Shafii katika Fat-h Al Aziz.

Lakini kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Hua haina haja kukosha sehemu ya Mnyama aliewindwa iliyoyafunwa na Mbwa wa Kuwindia, kwani ni *Ummu ul Balwa* (Kitu kinachodharauliwa hukmu yake juu yake),ambapo huu ni mmoja kati ya Mitizamo ya Madhhab ya Imam Al Shafii juu ya Jambo hili.'***(Al Majmuu Fi Sharh Al Muhadhhab)*

Lakini kwa Upande wa Imam Al Muhaqqiqin Al Faqih Imam Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii Al Makki basi yeye anasema kua: '**Sehemu aliyotafuna Mbwa kwa Mnyama aliemuwinda hua ni yenye Najis Mughallazah, kama vile inavyokua sehemu yeyote itakayotafunwa na Mbwa wakati ikiwa na Maji. Hivyo Mtizamo sahih ni kua Hua si *Ummu Ul Balwa* - haidharauliki kutokana na Upekee wake, hivyo hukmu sahih ni kua inabidi ikoshwe mara 7 kwa maji na mara moja miongoni mwao ikiwa kwa Mchanga.**

Na hua hakuna Ulazima wa Kuikata Nyama ya sehemu hio na Kuitupa, kwa sababu haikunukuliwa hivyo kwenye Hadith, ama kuhusiana na Mate yatakayokua yameingia ndani yake

hua hayana tatizo kwa sababu hua hakuna Najis ndani ya Nyama ya Mnyama husika kama ilivyoelezewa.' *(Tuhfah Al Muhtaj)*

Naam..baada ya kuangalia Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kuhusiana na Kutoruhusika Kufuga Mbwa bila ya Kua na Sababu inayokubalika Kisharia kama alivyosema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii kua: '**As-hab wa Madhhhab yetu wanakubaliana kua Ni Haram kufuga Mbwa bila ya Sababu inayokubalika Kisharia Yaani kwa mfano Mtu kuamua Kumfuga Mbwa kwa sababu ya kupenda Muonekano wake Mbwa huyo, au Kujionesha kwa Watu, n.k. Hivyo hii imeharamishwa na hakuna Utofauti wa Mtizamo Juu ya Hili.'***(Sharh Sahih Muslim)*

Hivyo Basi na tumalizie mada kwa kuangalia kuhusiana na Mitizamo ya Madhhab mengine juu ya Jambo hili.
Kwani anasema Muwaffaq Ad Din Imam Abu Muhammad Abd Allah Ibn Ahmad Ibn Muhammad Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Kisharia basi hua Inaruhusika Kumiliki na kutumia Vitu vyote vyenye Manufaa na kuruhusika Kuuza isipokua kile kilichokatazwa ndani ya Vyanzo vya Sharia za Kiislam. Kwa mfano kama Mbwa asietumika kwa ajili ya Uwindaji, Mtumwa mwenye Mtoto Mchanga na Wakfu uliokwisha Andikwa na kuwekwa.'*(***Al Mughni Sharh Mukhtasar Al Khiraqi)*

Ambapo kwa upande wa Imam Yusuf Al Hadi Al Hanbali kua: **'Bila ya Shaka *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameruhusu Kufuga Mbwa wa Kuwindia katika Hadith kadhaa, na akasema kua Kufunga Mbwa wa Kuwindia hua hakumpunguzii Mtu Thawabu. Na katika Hadith nyengine akaruhusu Kufuga Mbwa kwa ajili ya Kulindia Mifugo, na hadith nyengine kwa ajili ya Kulindia Kondoo na Nyengine kwa ajili ya Kulinda Shamba.**

Hivyo basi hua inajulikana sababu ya kuruhusika Kufuga Mbwa ni kutokana Makusudio maalum, na hukumu yake hutegemeana na kuwepo kwa sababu husika ama la. Hivyo kama sababu husika ipo basi itakua inaruhusika,mbali ya kua baadhi ya sababu ni nzito zaidi ya sababu za Kilimo Shambani, na sababu nyengine kua ni sawa na sababu zilizotajwa katika Vyanzo vya Sharia. Hivyo bila ya shaka Mazao hua na hukumu sawa na Mashamba, Ng'ombe hua sawa na Kondoo,Kuku na Mabata pia Na hivyo Malengo hua ni kuwaweka Mbwa Mwitu mbali na Mifugo ya mtu husika, na hivyo Hukmu yake hua ni sawa na Hukmu ya Ulinzi wa Mifugo.

Na bila ya shaka Khofu ya Majambazi hutoa Malengo ya Kufuga Mbwa kwa ajili ya Kumtahadharisha Mtu na kumuamsha hua ni Sababu Muhimu Zaidi. Hivyo Muumba alieweka Sharia ametilia Maanani juu ya Kuleta Manufaa na Kuepusha Madhara, hivyo kama ikiwa hakuna sababu basi hua ni Kosa Kufuga Mbwa.'*(Al Ighrab Fi Ahkam Al Kilab)*

Ambapo kwa upande wa Madhhab ya Imam Ahu Hanifa basi tunaona kua anasema Imam Abd Allah Ibn Ahmad An Nasafi Al Hanafi kua: **'Mbwa si Mnyama ambae ni Najis Al Ain yaani Kila kitu chake ni Najis, kwa sababu ni Mnyama ambae ana Manufaa kwa mfano katika Kulinda Mifugo, Shamba na pia Kuwindia, na Sharia inaonesha wazi kua Mbwa wa Kuwindia atakapomkamata Mnyama anaemuwinda basi hua ni halali kumla Mnyama huyo.**

Na Ingawa kwenye hadith imethubitishwa kua Mdomo wake, Mate yake, Kinyesi chake n.k kua ni Najis, lakini hata hivyo haiwezekani kufanya Makisio kutokana na hukmu hii kua kila kitu chake Mbwa ni Najis.'*(Al Bahr Raiq Sharh Kanz Al Daqaiq)*

Na hivyo kwa upande wa Amin Al Fatwa Imam Muhammad Aala Ad Din Al Husayni Al Khalwati Al Hanafi basi anasema kua: '**Katika Madhhab yetu ya Hanafi hua ni Makruh Tahrima - Katazo linalokirihisha kufuga Mbwa kama Mnyama wa Kufuga tu, lakini hua inakubalika Kufuga Mbwa kwa ajili ya Uwindaji na Ulinzi wa Mali, Mifugo, Shamba n.k.'***(Al Hidaya Al Aaliyah)*

Katika kuangalia Upande wa Mtizamo wa Madhhab ya Imam Malik kuhusiana na Kufuga Mbwa na wacha tuanze na uthibitisho wa Hadith yetu isemayo kua: '**Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: Yeyote yule atakaefuga Mbwa asiekua wa Kuwindia, wala kulindia Wanyama au Shambani basi atafutiwa Qirat mbili za Malipo Ya Mema yake ya Kila Sik**u.'*(Sahih Muslim)*

Na tunapomuagalia Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Qurtubi Al Maliki ambae ni Mwanazuoni Mahiri wa Hadith na Fiqh wa Madhhab ya Imam Malik, na pia ni Mtaalamu mkubwa sana wa Ilm ya Makubaliano ya Ijmaa za Wanazuoni wa Kiislam tangua kuanzia kwa Masahaba *Radhi Allahu Anhum*, ambapo kwa upande mmoja basi tunaweza Kumfananisha na Imam An Nawawi na kusema kua Imam Ibn Abd Al Barr ni Imam An Nawawi wa Madhhab ya Imam Malik.

Naam..hivyo Imam Ibn Abd Al Barri anaifafanua Hadith hii tuliyoanza nayo kwa upande wa Mtizamo wa Fiqh ya Madhhab ya Imam Malik kwa kusema kua: '**Hadith hii inaonesha kua Kufuga Mbwa hua si Haram hata kama ikiwa kuwafuga huko ni kwa ajili ya sababu nyenginezo zaidi ya zilizotajwa kwenye Hadith hii yaani Kuwindia na Kukindia.**

Na hii ni kwa sababu Maneno yasemayo "Atapunguziwa Qirat mbili kutoka katika amali zake njema Za Kila Siku" kunamaanisha kua Inaruhusika, na haijakatazwa,kwa sababu haiwezekani kua katika kukataza kitu fulani basi isemwe kua Atakefanya kitu husika basi atapunguziwa Malipo yake kutoka katika amali njema zake.

Bali kama ingeharamishwa basi Muumba alieweka Sharia angebainisha wazi juu yake ili Waislam wasifanye Jambo hilo. Na hivyo maneno haya yanamaanisha kua kufanya Hivyo hua hajupendekezwi na kunakirihisha, lakini si haramu*(Al Istidhkar)*

Ambapo hata hivyo hoja hii ya Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik imejibiwa na Al Hafidh Imam Zayn Ad Din Abd Rahman Al Iraqi Al Qurdi Al Shafii ambae amesema kua: '**Mtizamo wake huu Ibn Abd Al Barri ni wa kushangaza sana, kwa sababu Hitimisho letu sisi la kua kufuga Mbaa ni Haram linatokana na Matokeo yake ambayo ni Mtu Kufutiwa Malipo ya Amali njema, na hivyo hii inaonesha kua Mtu husika amefanya jambo lililoharamishwa, na hivyo kumfutia Thawabu zake Za Amali njema zake kama vile ambavyo zinavyofutwa thawabu za Ibada ya Sala kwa anaekunywa Ulevi,au Mtumwa aliemkimbia Bwana wake, au anaenda kwa Mpiga Ramli, n.k, na hivyo hii kumaanisha kua Kitendo husika kimeharamishwa, kwani ni kutokana na kuharamishwa kwake basi ndio maana ikawa Mtu anafutiwa Thawabu zake.**

Na bila ya shaka sababu iliyodhihirishwa ndani ya Hadith iko wazi kua kufutwa kwa Malipo ya Mali njema kunatokana na Dhambi iliyofanywa. *(Tarh Al Tathrib)*

Na Mujaddid Ad Din Al Hafidh Al Asr Shaykh Ul Islami Imam Abu Fadhl Ahmad Ibn Ali Ibn Muhammad Ibn Ali Ibn Mahmud Ibn Hajar Al Asqalani Al Shafii nae pia amejibu hoja ya Imam Ibn Abd Al Barr kwa kusema kua: '**Kinachodaiwa kua si haram kulingana na Hoja aliyoieleza Ibn Abd Al Barr, si chenye kusimamia katika Msingi wowote. Bali inawezekana kua adhabu inayokuja kutokana na kufuga Mbwa hua ni katika hali ya kutowezekana kwa Mtu Kuweza kufanya Mema yenye thamani ya Qirat ya Amali njema zake alizokua akizifanya pale alipokua hafugi Mbwa.**

Na hivyo inawezekana kua Kufuga Mbwa ni Haram na hii ni kutoka na matokeo ya Mtu kufutiwa Thawabu kutokana na Dhambi ya Kufuga Mbwa ambayo hua ni sawa na Qirat mbili za Malipo. Hivyo kile anachofutiwa Mtu anaefuga Mbwa kutoka katika amali njema zake hua ni sawa na Dhambi iliyotokana na Mfugaji Mbwa husika, ambacho ni Qirat mbili.'*(Fat-h Al Barr)*

Kwani mbali ya Uthibitisho wa Hadith hio kutumiwa na Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik juu ya Kuruhusika kufugwa kwa Mbwa kulingana na Mtizamo wao lakini pia Wanazuoni hao wanatumia *Aya ya Surat Al Maidah* 5:4 tuliyoiangalia hapo kabla Kuhusiana na kuruhusika Kutumia Mbwa kwa ajili ya Kuwindia.

Na hivyo kulingana na **Mtizamo wa Imam Malik mwenyewe na Imam Al Zuhri basi wanasema kua: Kama Mate ya Mbwa ingekua Ni Najis basi Isingeruhusika Kuliwa kile walichokikamata kwa Mdomo wao, hivyo kuruhusika kuliwa kwake kunamaanisha kua Mate yao ni Tohara.'***(Imam Muhammad Ibn Said Ibn Habbib Ibn Sahnun Al Maliki katika Mudawaanah Al Kubra)*

Na pia kuna Hadith isemayo kua:

وَقَالَ أَحْمَدُ بْنُ شَبِيبٍ حَدَّثَنَا أَبِي، عَنْ يُونُسَ، عَنِ ابْنِ شِهَابٍ، قَالَ حَدَّثَنِي حَمْزَةُ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، عَنْ أَبِيهِ، قَالَ كَانَتِ الْكِلاَبُ تَبُولُ وَتُقْبِلُ وَتُدْبِرُ فِي الْمَسْجِدِ فِي زَمَانِ رَسُولِ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فَلَمْ يَكُونُوا يَرُشُّونَ شَيْئًا مِنْ ذَلِكَ.

Amesema Ahmad Ibn Shabib kuaamesema Baba yangu kua amesema Yunus kua amesema Ibn Shihab kua amesema Hamza Ibn Abd Allahi kua amesema Baba yake ambae ni Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: Mbwa walikua wakija na kuondoka na Kukojoa Msikini, katika Wakati wa Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na ilikua Mkojo wao haumwagiwi Maji.'*(Sahih Bukhari)*

Na hivyo anasema Imam Abu Al Hasan Ali Ibn Khallaf Ibn Abd Al Malik Ibn Al Battal Al Baqri Al Andalus Al Qurtubi Al Maliki anasema kuhusiana na Hadith hii kua: '**Kwa Mbwa kuingia na kutoka Msikitini hua kunajumuisha na Kupangusa na Pua zao pia, Kunywa Maji na Kula Vyakula vilivyobakia bakia, kwa sababu Miskiti ilikua ni sehemu pia ya Kulalia Wasafiri Wageni na Wajumbe wa Kigeni pia.**

Na Masahaba wa Ahl Al Sufa pia walikua wakiishi ndani yake Hivyo kama Mbwa si Tohara basi wasingeruhusiwa kuingia hata Miskitini, kwa sababu Waislam wanakubaliana kua Haikubaliki kwa Najis kuingia Msikitini. Hivyo Mbwa kua wanaingia na Kutoka kunamaanisha kua kitendo hicho kilikua kikirudiwa na Mbwa hao Kuingia Msikitini na kutozuiwa kwao kunamaanisha kua Hawana Najis, kwa Sababu Viumbe hua hawawi Najis.'*(Sharh Ibn Battal)*

Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqalani Al Shafii amejibu hoja hii pia kwa kusema kua: '**Jambo ambalo tunaweza kusema kuhusiana na hadith hii ni kua Hali hii ilikua hapo mwanzoni mwa Uislam, kulingana na kanuni ya kuruhusika kwake, na hivyo baadae likaja amrisho la Kuiheshimu na akuitukuza Miskiti, Kuitoharisha, na Kutia Milango.**

Na hili kinadhihirishwa na Ismail Al Bukhari ambae yeye ameongezea katika Hadith Ya Ibn Wahb ambae amesema kua: Umar alikua akinadia kwa sauti yake ya juu kabisa kua: Epukeni Mazungumzo yasiyokua na Maana Miskitini. Na Ibn Umar amesema kua Nilikua nikilala

Msikitini katika Wakati wa Uhai wa *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam,* na kulikua kuna Mbwa wanakuja na kutoka, n.k.

Na hivyo hii inaonesha kua Tukio hili lilikua kabla ya amrisho la Kuiheshimu Miskiti, na pia juu ya Maneno ya Kipuuzi Msikitini.'*(Fat-h Al Barr)*

MUBTILAT SALAT – JEE INARUHUSIKA KUUZA NA KUNUNUA MBWA

❖❖❖❖

Naam..baada ya kuangalia Mitizamo tofauti juu ya Ufugaji wa Mbwa wenye Kunufaisha katika Uislam kulingana na Madhhab tofauti basi kuna Suali ambalo baadhi wanaweza Kujiuliza ambalo ni kua: '**Mbwa haruuusiki Kufugwa isipokua Mwenye Manufaa na Kama inaruhusika Kufuga Mbwa kulingana na Manufaa yake, basi Jee inaruhusika pia Kuwauza ama La?**

Na Suali hili linaulizika kwa sababu ya kua hapo Kabla tulifafanua Hadith isemayo kua:

عن أَبِي هريرة أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: إِنَّ اللَّهَ حرم الخمر وثمنها، وحرَّم الميتة وثمنها، وحرم الخنزير وثمنه

Amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: *Allah Subhanah wa Ta'ala* ameharamisha Mbwa na Bei yao, Ameharamisha Nguruwe na Bei Yake, na ameharamisha Ulevi na Bei Yake.' *(Jamii Sahih, Al Awsat, Al Hawi Al Kabir)*

Kwani tunapoliangalia Suali hili basi tunaona kua kwa Upande wa Madhhab Ya Imam Al Shafii Na Madhhab ya Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: '**Haikubaliki Kuuza na Kununua Mbwa iwe Mbwa huyo ni Mwenye Manufaa ama la, na hii ni kutokana na Uthibitisho wa Hadith ya Ahu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* iliyoharamisha Bei ya Mbwa**.'*(Mawsuah Fiqhiyyah)*

Kwani anasema Imam Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali kua: '**Hakuna tofauti ya Mtizamo katika Madhhab yetu ya Imam Ahmad kua Biashara ya Mbwa yeyote hua ni Haram, na huo ndio Mtizamo wa Imam Hasan Al Basr, Imam Rabiah, Imam Hamad, na Imam Al Shafii, Imam al Awzai, Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* wao wanachukia Biashara ya Mbwa**.'*(Al Mughni)*

Ambapo kwa Upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii basi yeye amesema kua: '**Ama kuhusiana na Kuharamishwa bei ya Mbwa ni kutokana na kua ni Njia mbaya na Chafu kabisa ya kujipatia Kipato. Hivyo Bei yake imeharamishwa, na Biashara yake hua Haram na hakuna fidiya kwa atakaeoharibu Biashara hio, iwe Mbwa huyo amefunzwa ama la, iwe ameruhusiwa kufugwa ama la, na huo ndio Mtizamo wa wengi miongoni mwa Wanazuoni akiwema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu*, Imam Hasan Al Basr, Imam Al Awzai, Imam Al Shafii, Imam Al Hakim, Imam Ibn Al Mundhiri n.k.**'*(Sharh Sahih Muslim)*

Na pia akasema Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii kua: '**Katazo la Dhahiri katika Hadith hii ni Haramisho la Kuuza na kununua Mbwa, ambalo ni jumuisho la kila aina ya Mbwa, iwe Mbwa wa kufugwa ama la, Mbwa aliefundishwa ama la, na hakuna madhara kama Mtu akiharibu biashara ya Mbwa.'***(Fat-h Al Barri)*

Na tunaoangalia kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa na Madhhab ya Imam Malik basi tunaona kua wao wanasema kua: Inaruhusika kuuza Mbwa Mwenye Manufaa kama ya Kuwindia na kulindia *Mawsuah Fiqhiyyah* Na kama ilivyotajwa katika *Fatawwa Al Hindiyah* kua: **Ama kuhusiana na Kuuza na kununua Mbwa, basi Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Anu Hanifa wanasema kua Awe Mbwa aliefugwa na Kufunzwa, au Mbwa atakaeweza Kufunzwa kwa ajili ya Malengo maalum, hivyo kama ikiwa Mbwa husika hakufunzwa wala hana uwezo wa kufundishika basi haitoruhusika Kuuzwa wala kununua.**'*(Fatawwa Al Hindiyyah)*

Ambapo kwa upande wa Wanazuoni wa Madhhab ya Imam Malik basi anasema Imam Ahmad Ibn Ghunaym Al Nafrawi Al Maliki kua: '**Hairuhusiki Kufuga Mbwa ambae haruhusiki Kufugwa katika Uislam. Ama kuhusiana na Wanaoruhusika Kufuga hua basi hua kuna Mitizamo mitatu juu yake ambayo ni:**

1-Hairuhusiki Kuuza wala Kununua Mbwa

2-Ni Makruh Inakirihisha Kununua na Kuuza Mbwa

3-Inaruhusika Kuuza na Kununua Mbwa.'*(Mawsuah Al Fiqhiyyah)*

Ambapo Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii amesema kuhusiana na Mtizamo wa Imam Malik kua: '**Imam Al Qurtubi amesema kua Mtizamo unaokubalika zaidi katika Madhhab ya Imam Malik ni kua Mbalo ya Kua Inaruhusika Kufuga Mbwa na hua Inakirihisha Kuuza na Kununua Mbwa, lakini hata hivyo kama watu wakikubaliana kuuziana na kununua Mbwa basi Biashara hio hua ni Sahih na haina tatizo.'***(Fat-h Al Barr)*

Neno Khabutha kwa Kilugha hua linamaanisha Ardhi isiyokua na Rutba, Kitu Kibaya, Kiovu, Kichafu, Kisichokua na Thamani, Upotovu wa Kivitendo au wa Kimaneno.

Naam..tumeanza na neno Khabitha kwa sababu kuna Hadith inayohusiana na mada yetu isemayo kua :

حَدَّثَنَا مُوسَى بْنُ إِسْمَاعِيلَ، أَخْبَرَنَا أَبَانُ، عَنْ يَحْيَى، عَنْ إِبْرَاهِيمَ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، - يَعْنِي ابْنَ قَارِظٍ - عَنِ السَّائِبِ بْنِ يَزِيدَ، عَنْ رَافِعِ بْنِ خَدِيجٍ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ "كَسْبُ الْحَجَّامِ خَبِيثٌ وَثَمَنُ الْكَلْبِ خَبِيثٌ وَمَهْرُ الْبَغِيِّ خَبِيثٌ" .

'Amesema Musa Ibn Ismail kua amesema Baba yetu kua amesema Yayha kua amesema Ibrahim Ibn Abd Allahi yaani Ibna Qaridhiin kua amesema Saibi Ibn Yazid kua amesema Rafii Ibn Khadiij *Radhi Allahu Anhu* kua amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kichumo cha Anaefanya Hijama ni *Khabithu*n, Bei ya Mbwa ni *Khabithun* na Malipo anayolipwa Kahaba ni *Khabithun.*'*(Sahih Bukhari na Muslim)***

Ambapo anasema Imam Abu Isa Al Tirmidhii kuhusiana na Hadith hii baada ya kuinukuu kua: '**Hadith hii ya Rafii ni Hasan Hadith na ndio ambayo Hukmu yake hua inatumiwa na wengi miongoni mwa watu wenye Ilm, ambao huchukia Bei ya Mbwa na huu ndio Mtizamo wa Imam Al Shafii, Imam Ahmad Ibn Hanbal, Imam Is-haq Ibn Rahawayh n.k.**

Lakini baadhi ya Watu wenye Ilm pia hua ni wenye Kuruhusu bei ya Mbwa wa Kuwindia na Kulindia.'*(Jamii Tirmidhii)*

Na tunapoiangalia Hadith hii basi tunaona kua Imetaja Vitu Vitatu vyenye Sifa ya Kua ni *Khabithat* ambavyo ni Malipo ya Kufanya Hijama, Malipo ya Kuuza Mbwa na Malipo ya Kumhonga Kahaba.

Na kama tulivyoona kuhusiana na maana ya neno Khabitha basi bila ya shaka juu ya Kahaba kila kitu hua kiko wazi, ila jee ni vipi kuhusiana na Hijama na Mbwa?

Na ama kuhusiana na Hijama, basi kwa upande wa Imam Abu Hanifa, Imam Al Layth Ibn Saad na Imam Malik basi wao wanasema kua: **Inaruhusika Kumlipa Mfanyaji Hijama na wala si kua haipendekezwi Kama alivyosema Imam Al Bajji Al Maliki katika Sharh Maliki Muwwata kua: 'Imam Malik amesema kua Hakuna tatizo kumlipa anaefanya Hijama kwani mimi sioni ubaya wowote.**

Ambapo amesema Imam Al Qurtubi Al Maliki kua: Neno Khabithat lililotumika katika Hadith hii linamaanisha Mjumuisho wa Matumizi yake, na pia hutumika kumaanisha hali ya kua baina ya Uharam wa Kitu na Kutopendekezwa Kitu husika.'*(Fayd Al Qadir)*

Ambapo kwa Upande wa Imam Al Khattabi Al Maliki basi yeye amesema kua: **'Neno *Khabithat* kimaana hua linategemeana na Malengo na Makusudio katika Kauli Husika'***(Fayd Al Qadir)*

Ambapo kwa upande wa Imam Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Hanbal basi wao wanasema kua: **'Haipendezi kwa Mtu anaefanyia Watu Hijama kuchukua Malipo kama mfanyaji ni Mtu aliekua huru, lakini hamna tatizo kama Mtu huyo Mfanyaji akiwa ni Mtumwa Ambapo amesema Imam Ibn Al Qayyim Al Hanbali kua: Kichumo cha Anaefanya Hijama hua ni Khabithat, ambayo hua ni sawa na Khabithat ya Kula Vitunguu Thaumu na Vitunguu Maji, isipokua Vitunguu hua na Harufu Mbaya wakati Malipo ya Mpiga Chuku hua Ubaya wa Kichuma kwake.'***(Zaad Al Maad)*

Na imesemwa *katika Mawsuah Al Fiqhiyyah* kua: **'Wengi Miongoni ma Wanazuoni wa Jumhur ya Uislam wanasema kua Inaruhusika Kutoza Malipo ya Hijama, na hua ni halali.'** *(Mawsuah Fiqhiyyah)*

Na hii ni kutokana na Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا مُعَلَّى بْنُ أَسَدٍ، حَدَّثَنَا وُهَيْبٌ، عَنِ ابْنِ طَاوُسٍ، عَنْ أَبِيهِ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ ـ رضى الله عنهما ـ عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم احْتَجَمَ وَأَعْطَى الْحَجَّامَ أَجْرَهُ وَاسْتَعَطَ.

Amesema Mualan Ibn Asadi ambae amesema kua amesema Wuhayb kua amesema Abi Tawus kua amesema Baba yake kua amesema Ibn Abbas *Radi Allahu Anhu* kua; '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifanya Hijama na kisha akamlipa aliemfanyia Hijama na kisha akachukua *Su'ut* (Dawa ya Kutoa baridi inayonuswa ya kutoa baridi)'*(Sahih Bukhari)*

Na kuna hadith isemayo kua:

حَدَّثَنَا مُسَدَّدٌ، حَدَّثَنَا يَزِيدُ بْنُ زُرَيْعٍ، عَنْ خَالِدٍ، عَنْ عِكْرِمَةَ، عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ ـ رضى الله عنهما ـ قَالَ احْتَجَمَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم وَأَعْطَى الْحَجَّامَ أَجْرَهُ، وَلَوْ عَلِمَ كَرَاهِيَةً لَمْ يُعْطِهِ.

Amesema Musaddad kua amesema Yazid Ibn Zuraiah kua amesema Khalid kua amesema Ikrimah kua amesema Bahr Ul Ilm Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alifanyiwa Hijama na akamlipa aliemfanyia, hivyo kama ingekua ni Haram basi asingemlipa. *'(Sahih Bukhari na Muslim)*

Na pia kuna hadith isemayo kua;

حَدَّثَنَا آدَمُ، حَدَّثَنَا شُعْبَةُ، عَنْ حُمَيْدٍ الطَّوِيلِ، عَنْ أَنَسِ بْنِ مَالِكٍ ـ رضى الله عنه ـ قَالَ دَعَا النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم غُلاَمًا حَجَّامًا فَحَجَمَهُ، وَأَمَرَ لَهُ بِصَاعٍ أَوْ صَاعَيْنِ، أَوْ مُدٍّ أَوْ مُدَّيْنِ، وَكَلَّمَ فِيهِ فَخُفِّفَ مِنْ ضَرِيبَتِهِ.

Amesema Adam kua amesema Shuayb kua amesema Humayd Al Tawwili kua amesema Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu* kua: '*Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alituma aitiwe Mtumwa anaefanya kazi ya Hijama (Aitwae Abu Taybah) akamfanyia Hijama *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* na kisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akaamrisha kua (Abu Taybah *Radhi Allahu Anhu* ambae alikua ni Mtumwa) alipwe Pishi moja au mbili za Tende na kisha akamuamrisha Mmiliki wa Abu Taybah kua ampunguzie Ushuru.' *(Sahih Muslim)*

Na hivyo anasema Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi kua: **'Wanazuoni wametifautiana juu ya Malipo ya Mpigaji Hijama, kwani wengi miongoni mwa Wanazuoni wa Mwanzoni mwa Uislam wanasema kua Kuchuma kutokana na Kufanya Hijama ha Kulipwa hua si Halali iwe Mtu huyo awe ni alie huru au ni Mtumwa.**

Ambapo huu ndio Mtizamo Mashhur wa Imam Ahmad Ibn Hanbal, ambapo hata hivyo kuna Mtizamo wake Mmoja ambao umenukuliwa sehemu moja Na ndio pia Mtizamo aa Wanazuoni wa Hadith, ni kua Mtu aliekua Huru kupokea Pesa kama Malipo ya kufanyia Hijama Mtu hua ni Haram, lakini kama Mfanyaji huyo akiwa ni Mtumwa basi ni Halali na uthibitisho wao ni Hadith ya Anas Ibn Malik *Radhi Allahu Anhu.*

Na wengi miongoni mwa Wanazuoni wameegemeza Mtizamo wao katika Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu*, kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimlipa aliefanyia Hijama, hivyo kama ni haram Basi asingemlipa, na hivyo Wanazuoni wameifaham hadithi kua Katazo hilo la Kupokea peza za Kufanyia Hijama kua ni Makruh Tanzih, Kirihisho Lisilipondekezwa, na hivyo hadith kua ni nyenye kutia ari watu kutokua ni wenye Kufanya kazi zenye malipo madogo na hivyo kuunga mkono Tabia njema na Kufuatilia Kazi zenye Utaalam wa kipato Zaidi.

Hivyo kama ingekua ni haram kutoza malipo ya kufanyia Hijama basi *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* asingetofautisha baina ya Malipo ya Mtu aliekua huru na Mtumwa, kwa sababu hairuhusiki kwa Muislam kumlisha Mtumwa wake kile kilichokua Haramu.'*(Al Minhaj Sharh Sahih Muslim)*

Ambapo kwa upande wa Mujaddid Ad Din Imam Ibn Hajar Al Asqallani Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Wengi miongoni mwa Wanazuoni wana mtizamo wa kua kichumo cha Kufanyia Hijama hua ni halali, na hii ni kutokana na Hadith ya Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* iliyonukuliwa na Imam Bukhari na hivyo Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* anawahoji wale wanaosema kua kichumo cha Anaefanya Hijama si halali kwa kusema kua: Kama ingekua si Halali basi Rasul**

Allah Salallahu Alayhi wa Salam **asingemlipa aliemfanyia Hijama. Hivyo mbali ya kua Kazi ya Kufanya Hijama si kazi ambayo ni nzuri lakini kichumo chake ni halali.**

Na hivyo Wanazuoni wamechukulia Hoja hii ya Abd Allah Jbn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua ni *Makruh Tanzih*, na baadhi ya Wanazuoni wamesema kua katazo limebatilishwa, na kuna wasemao kua Malipo hua ni haram pale anaefanya Hijama anapokua ni Mtu aliekua Huru, lakinj akiwa ni Mtumwa basi hua ni Halali, na kuna wasemao kua hua ni haram pale inapokua kazi ya hijama hio haijawekwa wazi.'*(*Fat-h Al Barr)*

Kwa maana hio basi Kuhusiana na Hijama basi Hadith zinatuonesha kua Kumlipa anaefanya Hijama hua haipendekezwi, na bora Mtu asilipishe, ila si haram.

Kazi ya Kufanya Hijama si kazi ambayo inamthaminisha Mtu.

Kufanya Hijama bila ya Malipo hua ni kama kutoa Sadaka, hususan kwa Mtu mwenye shida ya Kufanyiwa.

Hivyo baada ya kuangalia kuhusiana na Bei ya Hijama basi tunaingia kwenye bei ya Mbwa na kulingana na Mtizamo sa Madhhab ya Imam Abu Hanifa basi anasema Imam Nur Ad Din Ahu Hasan Ali Ibn Sultan Muhammad Ibn Hirawi Al Qarri Al Hanafi maarufu kama Imam Mulla Ali Al Qari kua: 'Hadith ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* inayosema kua: 'Bei ya Mbwa ni *Khabithat*' imefafanuliwa na Imam Abu Hanifa ambae amesema kua: Neno *Habithat* halimaanishi kua ni Haram, bali linamaanisha kua si Tohara, sio Safi na hivyo kumaanisha kua ni Makruh.

Kwani *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ametumia neno hilo kwa Mtu anaelipwa kwa Kufanya Hijama pia, na hivyo hakuna hata mmoja aliesema kua kichumo cha Anaefanya Hijama kua ni Haram.'*(Al Mirqaat Sharh Mishkat)*

Mulla Ali Al Qarri Al Hanafi anaendelea kutuambia kua: **'Na pia Hadith inayosema kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* amekataza Bei ya Mbwa, basi kulingana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ni kua Katazo la Bei ya Mbwa lililotangaziwa katika Hadith lilitolewa katika kipindi ambacho *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alipoamrisha pia Kuuliwa kwa Mbwa, na hivyo katika kipindi hicho ilikua hairuhusiki kabisa kua na Mbwa Lakini baada ya hapo, ikaruhusiwa kua na Mbwa wenye Manufaa, na pia imenukuliwa kua Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam alimuamrisha Mtu alipe Fidya ya Dirham 40 baada ya Kumuua Mbwa wa Kuwindia, na akamuamrisha Mwengine alipe Fidia ya Kondoo baada ya Kumuua Mbwa wa Kulindia Mifugo.**

Hivyo Hadith hizi zinaonesha kua kuna Thamani juu ya Mbwa wa Kuwindia na wa Kulindia, na Hivyo Imam Abu Hanifa amehukumu kua inaruhusika Kuua na kununua Mbwa.' *(Al Mirqaat Sharh Mishkat)*

Na pia kwa upande wa Imam Muslim na Imam An Nasai basi amenukuu hadith ambayo ameipa Sifa ya kua ni Hadith Munkari semayo kua:

أَخْبَرَنِي إِبْرَاهِيمُ بْنُ الْحَسَنِ، قَالَ أَنْبَأَنَا حَجَّاجُ بْنُ مُحَمَّدٍ، عَنْ حَمَّادِ بْنِ سَلَمَةَ، عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ، عَنْ جَابِرِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم نَهَى عَنْ ثَمَنِ الْكَلْبِ وَالسِّنَّوْرِ إِلاَّ كَلْبَ صَيْدٍ . قَالَ أَبُو عَبْدِ الرَّحْمَنِ هَذَا مُنْكَرٌ .

‘Amesema Ibrahim Ibn Hasan kua amesema Hajjaj Ibn Muhammad kua amesema Hamamd Ibn Salamah kua amesema Abi Zubayr kua amesema Jabir Ibn Abd Allah *Radhi Allahu Anhu* kua: *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ameharamisha Bei ya Mbwa na Paka isipokua Mbwa wa Kuwindia.’*(Sahih Muslim, Sunnan An Nasai)*

Hivyo ingawa kwa upande wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa ambao Mtizamo wao ni kua inaruhusika kuuza na kununua Mbwa mwenye Manufaa basi wametumia vithibitisho vya Hadith hizi. Lakini kwa upande mwengine basi hii haimaaniahi kua Hata Mbwa anaetumika kwenye Mashindano ya Mbio za Mbwa kua inaruhusika kuuzwa na Kununuliwa kutokana na Manufaa yake.

Na hii ni kwa sababu kwanza Mchezo wa Mashindano ya Mbio za Mbwa hua ni wa Kamari, hivyo Wanazuoni Wote wanakubaliana kua ni Haram kucheza Kamari. Na pili ni kwa sababu Mbwa wa Mashindano hua anahitaji usimamizi wenye Matumizi maalum kwa ajili yake na hivyo hua ni sawa na kutumia Mali na Wakati kwa Malengo yaliyokatazwa katika Uislam.

Na amesema Imam Daud kua:

حَدَّثَنَا الرَّبِيعُ بْنُ نَافِعٍ أَبُو تَوْبَةَ، حَدَّثَنَا عُبَيْدُ اللَّهِ، - يَعْنِي ابْنَ عَمْرٍو - عَنْ عَبْدِ الْكَرِيمِ، عَنْ قَيْسِ بْنِ حَبْتَرٍ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عَبَّاسٍ، قَالَ نَهَى رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم عَنْ ثَمَنِ الْكَلْبِ وَإِنْ جَاءَ يَطْلُبُ ثَمَنَ الْكَلْبِ فَامْلأْ كَفَّهُ تُرَابًا .

Kwani amesema Rabiu Ibn Nafii Abu Tawbat kua amesema Abd Allahi yaani Ibn Amri kua amesema Abd Al Karim kua amesema Qays Ibn Habtar kua amesema Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* kua: ‘**Ameharamisha *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* bei ya Mbwa, Hivyo akija Mtu Kuulizia bei yake basi Kijaze Kiganja chake na Mchanga.**’ *(Sunnan Abu Daud)*

Ambapo maneno yasemayo kua Kijaze Kiganja cha Mtu anaetaka kununua Mbwa kwa Vumbi yanamaanisha kua Usimpe au Usimtekelezee kile anachokitaka. Na kama tulivyoona hapo kabla kuhusiana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Abu Hanifa, kua inakubalika Kuuza Mbwa mwenye Manufaa.

Lakini kwa upande wa Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi basi yeye anasema kua: ‘**Ama kuhusiana na Bei ya Mbwa, na kuhusiana na kua ni Moja Kati ya Njia mbaya kabisa na Chafu za Kujipatika Riziki, na hivyo hii inamaanisha kua Imeharamishwa Biashara yake, na atakaefanya hivyo hua hastahiki malipo yake iwe Mbwa huyo ni Mwenye Manufaa ama la, amefunzwa ama la, na huu ndio Mtizamo wa wengi Miongoni mwa Wanazuoni akiwemo Abu Hurayrah Radhi Allahu Anhu, Imam Hasan Al Basr, Imam Rabiah, Imam Al Awzai, Imam Al Hakim, Imam Hamad, Imam Al Shafii, Imam Abu Daud, Imam Ahmad, Imam Ibn Al Mundhiri n.k**

Ambapo Imam Abu Hanifa amesema kua Mbwa mwenye Manufaa anaruhusika Kuuzwa na Malipo yake anatakiwa kupewa aliewafunza. Na pia Imam Ibn Al Mundhiri amenukuu kutoka kwa Imam Jabir, kwa Imam Ataa na Imam Ibrahim An Nakhai kua inaruhusika kuuza na kununua Mbwa wa Kuwindia tu.

Na kuna Nukuu kwa Imam Malik, ambapo moja wapo inasema kua, hairuhusiki Kuuza isipokua Thamani ya Malipo anaruhusika kupewa aliemfunza Mbwa husika Na mtizamo wa pili ni kua Inaruhusika Kuuza na Kumlipa aliemfunza Mbwa.

Na mtizamo wa Tatu ni kua hairuhusiki Kuuza wala Kumlipa aliemfunza Mbwa. **Na uthibitisho wa wenye Mtizamo huu ni Hadith iliyosema kua Hairuhusiki Kuuza Mbwa isipokua wa Kuwindia, na hadith nyengine imesema isipokua kwa Mbwa wa Kulindia**. **Na kua Uthman Ibn Affan *Radhi Allahu Anhu* alimlipisha Mtu Fidia ya Ngamia 20 kwa sababu ya Mbwa aliemuua.**

Na Amr Ibn Al Aas *Radhi Allahu Anhu* alimlipisha Mtu Fidya baada ya kumuua Mbwa wa Kulindia, lakini Nukuu hizi zote ni dhaifu kulingana na Makubaliano ya Wanazuoni wa Hadith, nami Nimeelezea haya katika Al Majmuu katika Mlango wa vinavyoruhusika Kuuza na Kununua.

Na *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salama* amekataza Bei ya Mbwa na kusema kua Kama ikiwa Mtu atakuja Kuulizia Bei yake basi Kijaze Kiganja chake na Vumbi Na hii ni Hadith ambayo imenukuliwa na Abd Allah Ibn Abbas *Radhi Allahu Anhu* ikiwa na Usahih, na Imam Ahmad na Imam Abu Daud wamesema kua Huu ni uthibitisho wa Kutokukubalika kuuza Mbwa na hivyo Mtu akija kuuliza basi asipewe Bei yake. Mbwa ni Mnyama Mchafu na haruhusiki Kuuzwa wala kununuliwa yaani kama Nguruwe kuhusiana juu ya hili.'*(Sharh Al Umdah)***

Na anasema Imam Ahmad Ibn Muhammad Ibn Abu Bakr Ibn Abd Al Malik Ibn Al Zayn Ahmad Ibn Jamal Ibn Muhammad Ibn Safii Ibn Muhammad Ibn Majid Husayn Ibn Taj Ali Ibn Maymun Al Qastallani Al Shafii kua**:** '**Kauli ya *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* ni Katazo la Bei ya Mbwa iwe Mbwa huyo aliefunzwa ama la, na hii ni kutokana na Uchafu wao, lakini kwa upande wa Hanafi na Maliki basi wanasema kua Inaruhusika Kuuza Mbwa wenye Manufaa.'***(Irshad Sari)***

Na Imam Taqi Ad Din Muhammad Ibn Ali Ibn Wahb Al Qushayri Al Manfaluti Ibn Daqqiq Al Id Al Shafii anasema kua: '**Wanazuoni wametofautiana kuhusiana na kuuza Mbwa waliofunzwa, ambapo kwa wale wanaowahesabu kua Ni Najis, yaani Imam Al Shafii basi yeye amekataza kabisa kabisa kuwauza na Hukmu hii ni kwa Mbwa wote.**

Ambapo wale wanaowahesabu kua ni Tohara basi wametofautiana juu ya kuwauza Mbwa waliofunzwa, kwa sababu kulingana na Mtizamo wao basi ni kua hukmu ya katazo juu yao hua haliwahusu mbwa wote.' *(Ihkam Al Ahkam)*

Na Imam Abu Hafs Umar Ibn Ali Ibn Ahmad Ibn Mulaqiin Al Andalus Al Ansari Al Shafii basi yeye anasema kua: **'Katazo la bei ya Mbwa linajumuisha Mbwa wote. Lakini Imam Ibn At Tin amesema kua Kuna aina mbili za Mbwa, aina ya kwanza ni Mbwa wa Kuwindia na Kulindia ambao kuna Mtizamo tofauti juu ya bei yao.**

Na kisha kuna Mbwa wengine wasiokua na Manufaa ambao hairuhusiki kuwafuga kwa sababu wanatisha na kudhuru watu na hivyo Bei yake imeharamishwa.'

Na tunafunga Mada ya Mbwa na Uharamu wake na Najis yake na yaliyoruhusika juu yake kwa kukumbushana maneno ya Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qalyubi Al Masri Al Shafii kua: '**Hua ni sahih kukubaliana na Manufaa ambayo yanayoweza kupatikana kutokana na Mbwa au hata Kinyesi, na hivyo Malipo ya Pesa yatakayopatikana Hua ni kutokana na Kuachana na Umiliki wa Kitu husika na wala hayatokua ni kutokana na Faida ya Bei ya Malipo ya kitu husika.'***(Hashiyah Al Qalyubi)*

Yaani kulingana na Mtizamo huu basi tunaona kua kutokana na Mtizamo wa Madhhab ya Imam Al Shafii kua Malipo ya Bei ya Mbwa hua ni Haram basi hua inaruhusika kwa Mtu kuachana na Mbwa wake kwa kumpa Mtu mwengine, ambapo Mtu huyo atatoa kiasi ya Malipo ya Pesa ambazo zitakua zinahesabika kama Fidia, na sio Bei.

Kwani hii hua inaruhusika kwa sababu Kiislam hua hairuhusiki Kuwanyanyasa Wanyama, wachia mbalo kuwaua bila sababu ya kua watasababisha madhara kama zinavyosema Hadith kua:

وَحَدَّثَنِي عَنْ مَالِكٍ، عَنْ سُمَيٍّ، مَوْلَى أَبِي بَكْرٍ عَنْ أَبِي صَالِحٍ السَّمَّانِ، عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " بَيْنَمَا رَجُلٌ يَمْشِي بِطَرِيقٍ إِذِ اشْتَدَّ عَلَيْهِ الْعَطَشُ فَوَجَدَ بِئْرًا فَنَزَلَ فِيهَا فَشَرِبَ وَخَرَجَ فَإِذَا كَلْبٌ يَلْهَثُ يَأْكُلُ الثَّرَى مِنَ الْعَطَشِ فَقَالَ الرَّجُلُ لَقَدْ بَلَغَ هَذَا الْكَلْبَ مِنَ الْعَطَشِ مِثْلُ الَّذِي بَلَغَ مِنِّي فَنَزَلَ الْبِئْرَ فَمَلأَ خُفَّهُ ثُمَّ أَمْسَكَهُ بِفِيهِ حَتَّى رَقِيَ فَسَقَى الْكَلْبَ فَشَكَرَ اللَّهُ لَهُ فَغَفَرَ لَهُ " . فَقَالُوا يَا رَسُولَ اللَّهِ وَإِنَّ لَنَا فِي الْبَهَائِمِ لأَجْرًا فَقَالَ " فِي كُلِّ ذَاتِ كَبِدٍ رَطْبَةٍ أَجْرٌ "

Amesema Malik kua amesema Sumayyi kua amesema Mawla Ibn Abi Bakri kua amesema Abi Salih Al Samani kua amesemakua amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: amesema *Rasul Allahi Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna Mtu alikua safarini njiani na akakutwa na Kiu kubwa sana,na mara akakutana na Kisima.

Hivyo akaingia ndani yake na kisha akanywa Maji na kisha akatoka Baada ya kutoka akamuona Mbwa ambae yuko taabani kwa Kiu kiasi ya kua alikua anaramba Matope. Hivyo yule Mtu akajiambia ndani ya Nafsi yake kua Huyu Mbwa anaadhibika kama nilivyokua nikiadhibika mimi kwa kiu.

Hivyo akarudi tena Kisimani na kuchote Maji kwa kutumia Kiatu chake na kisha akabana kwa Meno yake na akaja nayo juu, na kumpa Maji hayo Yule Mbwa. Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* akamshukuru Mtu huyo kwa Jema hilo alilolifanyakwa Mbwa huyo na Kumsamehe Dhambi zake.

Hivyo Masahaba *Radhi Allahu Anhum* wakaulizakwa kusema: Ya Rasul Allah! Jee kuna Malipo hata kwa kuwafanyia Mema Wanyama?

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* akasema: Naam..Kuna Malipo kwa Kumfanyia Mema kila mwenye Ini lenye Uhai** *(Malik Muwwata, Sahih Bukhari na Muslim)*

Na kuna hadith isemayo kua:

وَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «غُفِرَ لِامْرَأَةٍ مُومِسَةٍ مَرَّتْ بِكَلْبٍ عَلَى رَأْسِ رَكِيٍّ يَلْهَثُ كَادَ يَقْتُلُهُ الْعَطَشُ فَنَزَعَتْ خُفَّهَا فَأَوْثَقَتْهُ بِخِمَارِهَا فَنَزَعَتْ لَهُ مِنَ الْمَاءِ فَغُفِرَ لَهَا بِذَلِكَ» . قِيلَ: إِنَّ لَنَا فِي الْبَهَائِمِ أَجْرًا؟ قَالَ: «فِي كُلِّ ذَاتِ كبد رطبَة أجر

Na amesema Abu Hurayrah *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi* wa Salam kua: Mwanamke Muasi ambae alisamehewa na *Allah Subhanah wa Ta'ala,* kwa sababu ya kua alipita njiani akamuona Mbwa anahaha kwa Kiu pembeni ya Kisima kiasi ya jua Mbwa huyo alikua bado kidogo afe.

Hivyo akavua Kiatu chake kisha akakifunga wa Mtandio wake na kukitumbukiza Kisimani na kuchota Maji kwa ajili ya Mbwa huyo, na akasamehewa Na *Allah Subhanah wa Ta'ala* kwa sababu hio, Masahab wakasema : 'Jee tuna Malipo katika kuwafanyia mema Wanyama?'

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa* Salam akasema: 'Kuna Malipo Kwa Kila Mnyama mwenye Uhai.'** *(Sahih Bukhari)*

Na kuna hadith isemayo kua:

عن ابن عباس رضي الله عنهما قال: رأى رسول الله صلى الله عليه وسلم حمارًا موسوم الوجه، فأنكر ذلك؟ فقال: والله لا أسمه إلا أقصى شيء من الوجه، وأمر بحماره، فكوي في جاعرتيه، فهو أول من كوى الجاعرتين.

***Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alimuona Punda ambae alikua ametiwa Alama ya Kuchanjwa Usoni mwake, hivyo hakupendezewa na jambo hilo, na hivyo Abd Allah Ibn Abbas Radhi Allahu Anhu akasema kua: 'Wa Allahi mimi sitomtia Alama Mnyama kweny Uso wake', hivyo akaamrisha kutia alama kwenye Mapaja, na yeye ndie mtu wa kwanza kuwatia alama Wanyama kwenye Mapaja.** *(Sahih Muslim)*

Na kuna Hadith isemayo kua:

حَدَّثَنِي عَبْدُ اللَّهِ بْنُ مُحَمَّدِ بْنِ أَسْمَاءَ، حَدَّثَنَا جُوَيْرِيَةُ بْنُ أَسْمَاءَ، عَنْ نَافِعٍ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ ـ رضى الله عنهما ـ أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ " عُذِّبَتِ امْرَأَةٌ فِي هِرَّةٍ سَجَنَتْهَا حَتَّى مَاتَتْ، فَدَخَلَتْ فِيهَا النَّارَ، لاَ هِيَ أَطْعَمَتْهَا وَلاَ سَقَتْهَا إِذْ حَبَسَتْهَا، وَلاَ هِيَ تَرَكَتْهَا تَأْكُلُ مِنْ خَشَاشِ الأَرْضِ ".

Amesema Abd Alla Ibn Muhammad Ibn Asmai kua amesema Juwayriyat Ibn Asmau kua amesema Nafii kua amesema Abd Allah Ibn Umar *Radhi Allahu Anhu* kua: Amesema *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* kua: 'Kuna Mwanamke ambae ameingia Motoni kwa sababu ya Paka

ambae alikua nae na ikawa hakumpa Chakula wala hakumuachia apate Kula Vidudu vya Ardhini.'*(Sahih Bukhari na Muslim)*

حَدَّثَنَا مُحَمَّدُ بْنُ كَثِيرٍ، أَخْبَرَنَا سُفْيَانُ، عَنْ أَبِي الزُّبَيْرِ، عَنْ جَابِرٍ، أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم مُرَّ عَلَيْهِ بِحِمَارٍ قَدْ وُسِمَ فِي وَجْهِهِ فَقَالَ " أَمَا بَلَغَكُمْ أَنِّي قَدْ لَعَنْتُ مَنْ وَسَمَ الْبَهِيمَةَ فِي وَجْهِهَا أَوْ ضَرَبَهَا فِي وَجْهِهَا " . فَنَهَى عَنْ ذَلِكَ .

Amesema Muhammad Ibn Kathir kua amesema Sufyan kua amesema Abu Zubayr kua amesema Jabir *Radhi Allahu Anhu* kua *Rasul Allah Salallahu Alayhi wa Salam* alisema alipomuona Punda ambae ametiwa alama Usoni kua: 'Hivi Jee haijakufikieni nyinyi kua Mimi nimemlaani Mtu yule anaewatia Alama Wanyama kwenye Nyuso zao au kuwapiga kwenye Nyuso zao, kwani nimekataza hayo.'

Wa bil Allahi Taqfiq!

MARUDIO YA VITABU VILIVYOTUMIKA KATIKA KUANDAA KITABU HIKI

❖❖❖❖

Al Bayyan Fii Madhhab Shafii **-** Imam Abu Al-Hussein Yahya Al-Imrani Al Yamani Al Shafii
Al Iqna Fi Hal Al Faz Abi ShujaaImam Al Khatib Al Shirbini Al Shafii.
Al Hidaya Sharh Al Bidaya - Shaykh Ul Islami Burhan Ad Din Abu Hasan Ali Ibn Abdul Jalil Abu Bakr Ibn Khalil Abu Bakr Habib Al Marghinani Al Rashdani Al Hanafi.
Al Hawi Al Kabir Fi Fiqh Madhhab Al Shafii - Al Allamah Al Faqih Imam Ali Muhammad Ibn Habib Al Mawardi Al Shafii.
Al Hidaya Al Aaliya - Sayyid Imam Muhammad Amin Ibn Sayyid Umar Ibn Sayyid Ibn Abd Al Aziz Ibn Sayyid Ahmed Ibn Sayyid Abd Rahim Ibn Said Najmu Ad Din Ibn Sayyid Muhammad Salahu Ad Din Ash Shami Ibn Abidin Al Hanafi.
Al Mujam Al Awsat – Imam Abu Qasim Sulayman Ibn Ahmad In Ayub Ibn Mutayyir Ibn Lakhmi Ash Shami At Tabarani.
Al Mudawwanah - Imam Muhammad Ibn AhmadAl Sarakhasi Al Hanafi.
Al Mubdi Sharh Al Muqni **-** Imam Ibrahim Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Muflih Al Maqdisi Al Hanbal.
Al Muhadhdhab Fii Fiqh Al Imam Al Shafii **-** Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Ali Al Shirazi Al Firuzabad Al Shafii
Al Majmuu Sharh Al Muhadhdhab - Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii.
Al Risala - Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii.
Al Mustasfa – Hujjat ul Islami Mujaddid Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii Al Tusi.
Al Umm – Mujaddid Ad Din Imam Muhammad Idris Al Shafii.
Ahkam Al Ahkami Imam Taqi Ad Din Abu Al Fat-h Muhammad Ibn Ali In Wahb Ibn Muti Ibn Abi Ataa Ibn Daqiq Al Idd Al Shafii.
Al Tajriid - Imam Abu Al Hasan Ahmad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Ahmad Ibn Jafar Al Quduri Al Hanafi
Al Takrirat Al Sadida fi Masail Mufida - Imam Hasan Al Kaff Al Shafii.
Asna Al Matalib Fi Sharh Raudh Al Talib **-** Shaykh Ul Islami Al Faqih Imam Abu Yahya Zayn Ad Din Zakarriyah Al Ansari Al Shafii.
Al Madhur **-** Shaykh Ul Islami Imam Abu Abd Allah Badr Ad Din Muhammad Ibn Abd Allah Ibn Bahadir Al Zarkashi.
Al Mughni - Imam Ahmad Ibn Abd Rahman Ibn Qudamah Al Maqdisi Al Hanbali.
Al Mausu'ah Al Fiqhiyah Al Kuwaitiyah.
Al Minhaj Talibin - Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakariyyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii.
Al Mutammad fi Fiqh Al Shafii - Imam Muhammad Al Zuhayli.
Al Muwaffaqat - Imam Abu Is-haq Ibrahim Ibn Musa Al Shatibi Al Andalus Al Maliki.
Al Muwatta - *Imam Malik Ibn Anas.*
Al Tadhhib Fi Fiqh Al Imam Al Shafii **-** Imam Abu Muhammad Al Husayn Ibn Masud Ibn Muhammad Al Fara Al Baghawi Al Shafii)
At Tamhiid Sharh Malik Muwwata **-** Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki.
Al Tajriid **-** Imam Abu Al Hasan Ahmad Ibn Muhammad Ibn Muhammad Ibn Ahmad Ibn Jafar Al Quduri Al Hanafi.
Al Qawl Al Tamm fi Ahkam Al Ma'mum wa-l-Imam **-** Muhammad Ibn Ahmad Ibn Al Imad Al Aqfahsi Al Shafii.

Al Wasit Fii Sunnan,wa Al Ijmaa, wa Al Ikhtilafi - Mujtahid Imam Abu Bakr Muhammad Ibn Ibrahim Ibn Al Mundhir Al Nishapuri Al Shafii.

Awn Muabud Fii Sharh Sunnan Abi Daud - Imam Abi Abd Rahman Sharrafi Al Haqq Muhammad Ashraf Sadiq Al Adhiim Al Aabadii.

Bushra Al Karim *Imam Said Ba Ishni.*
Badai Al Sanai Fi Tartib Ash Sharai - Allamah Abu Bakar Alaa Din Ibn Masud Al Kasani Al Samarqandi Al Hanafi.
Badr al Munir - Imam Al Faqih Al Hafidh Siraj Ad Din Abu Hafs Ali Ibn Ahmad Ibn Al Mulaqiin Al Shafii Al Misri.
Bidayat Al Mujtahid -Imam Abu Al Walid Muhammad Ibn Ahmad Ibn Rushd Al Andalus Al Maliki.
Bushra Al Karim - Imam Abd Allah Al Jurdani Al Shafii.

Daqaiq Uuli Nuuha Sharh Muntaha Al Iraadat - Imam Al Buhuti Al Hanbali.

Fatawa Al Hindiyyah Fatawa Aalamgiriya Al maarufah Bi Al Fatawa Al Alamkiriyah Fi Madhhab Al ImamAl Azzam Abi Hanifa Al Nuuman.
Fatawa Fiqhiyyah Al Kubra - Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Makki Al Shafii.
Fat-h al Aziz - Imam Abu Qasim Ibn Muhammad Al Rafii Al Shafii.
Fat-h al Aalam Bi Sharh Murshid Al Anam –Imam Muhammad Ibn Abd allah Al Jurdani Al Masri Al Shafii.
Fathul Mu'in - Imam Zayn Ad Din Al Malibari.
Fiqh Islamiyy Wa Adilat- Imam Wahbah Mustafa al-Zuhayli.
Fiqh Al Manhaj aAla Madhhab Al Imam Al Shafii.Dr. Mustafa Al Khinn, Dr. Mustafa Al Bugha Na 'Ali Al Shurayhi.
Fiqh Aala Madhdhahib Arbaa - Imam Abd Rahman Al Jazari
Fiqh Al Ibadat Aala Madhhab Shafii - Hajjah Durriah Al-Aytah.
Fat-h Al Barr Bi Sahih Bukhari - Imam Abd Rahman Ibn Ahmad Ibn Rajab Al Hanbali.
Fat-h Al Barr Sharh Sahih Al Bukhari– Mujaddid Ad din Shaykh Ul Islami Al Hafidh Imam Shihab Ad Din Abu Fadhil Ahmad Ibn Nur Ad Din Ibn Ali Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani
Fat-h Al Barr Fi Al Tartib Fi Fiqhi Li Tamhid - Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Abd Al barr Maliki.
Futuhat Rabbaniyah –Al Hafidh Al Faqih Imam Muhammad Ibn Alan Al Sadiqi Al Shafii.

Hashiyyah Al Bujaraimi ala Sharh Minahj Al Tulab - Imam Sulaiman Ibn Muhammad Ibn Umar Al Bujaraimi Al Shafii.
Hashiyyah Al Jamal ala Sharh Minhaj - Imam Sulayman Ibn Umar Al Jamal Al Shafii.
Hashiyyah Al Bajuri- Imam Ibrahim Ibn Muhammad Ibn Ahmad Al Shafi Al Bajuri.
Hashiyyah Shabramilisi aAla Nihayat Al Muhtaj - Imam Nur Ad Din Ali Shabramilisi Al Shafii.
Hashiyyah Al Qalyubi aAla Sharh Ibn Qasim Al Ghazi - Imam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qalyubi Al Masri Al Shafii.
Hashiyyah Al Qalyubi 'Ala Sharh Al Muhalla 'Ala Minhaj Al TalibinImam Shihab Ad Din Ahmad Ibn Ahmad Ibn Salamah Al Qalyubi Al Masri Al Shafii.
Hashiyyah Ibn Abidin - Imam Muhammad Amin Ibn Amr Ibn Abd Al Aziz Ibn Aabidin Al Shaami Al Hanafi.
Hashiyyah Al Shirwani - Imam Abu Amr Uthman Ibn Abd Rahman Salah Ad Din Al Kurdi Al Sharhazuri Al Shafii.
Hashiyyah As Safti - *Imam Yusuf As Safti Al Maliki..*
Hashiyyah Al Sharwani aAla Tuhfah Al Muhtaj - Imam Abd Al Hamid Al Sharwani Al Shafii.

Hawashi Al Sharwani Wa Al Abbadi aAla Tuhfah Muhtaj Bi Sharh Minhaj -Imam Abdul Hamid Al Makki Al Sharwani Al Shafii na Imam Ahmad Ibn Qasim Al Abbadi Al Shafii

I'aanat at-Taalibin 'ala Hal Alfaadh Fath al-Mu'een – Imam Uthman Ibn Shata, Abu Bakr al Bakri.
Ihya Ulum Ad Din - Hujjat ul Islami Mujaddid Ad Din Imam Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al Ghazali Al Shafii Al Tusi.
Irshad Sarri ala Sharh Sahih Bukhari wa Imam Ahmad Ibn Muhammad Al Qastallani Al Shafii

Kashaaf Al Qinaa Al Muhaqiq - Imam Mansur Ibn Yunus Al Buhuti Al Hanbali.
Kitab Al Istidhkar li Madhhab Ulama Al Amsar Fi Ma Tadamanahu Al Muwwata min Maa'ani wa al Ray wa Al Athar - Imam Yusuf Ibn Abd Allah Ibn Muhammad Ibn Abd Al Barr Al Andalus Al Qurtubi al Maliki

Mawsuat Al Fiqh Al Islami wa Adilat - Imam Wahba Al Zuhayly.
Matalib Uli Nuha - Al Allamah Al Qadhi Al Imam Mustafa Ibn Saad Ibn Abduh Al Suyuti Al Ruhaybani Ad Dimashq Al Hanbali.
Maraqi Al Falah - Imam Ali Shurunbulali.
Mughni Al Muhtaj Ila Ma'rifah Ma'ani Al Fazd Minhaj - Al Khatib As- Shirbini, Shamsuddin Ibn Muhammad.
Minhaj Al Thalibin wa Umdatun Muftin fi Fiqh –Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriayah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi Al Shafii.
Musnad Imam Ahmad *Imam Ahmad Ibn Hanbal.*
Musanaf Ibn Abd Razzak – Imam **Abd** Al **Razzaq Ibn** Hammam Ibn Nafi' Al San'ani
Musanaf Ibn Abu Shaybah Imam Abu ShaybahAbū Bakr ʿAbd Allāh Ibn Muḥammad Ibn Abī Shaybah Ibrāhīm Ibn ʿUthmān Al ʿAbasī Al Kūfī
Mustadrak Al Hakim, Al Mustadrak 'ala Al Sahihayn- Abu Abd Allah Muhammad Ibn Abd Allah Al Hakim Al Nishapuri

Nihyayat Al Muhtaj bi Sharh Al Minhaj - Imam Al Shafii Al Saghir Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Ibn Hamza Al Ramli.
Nayl Al Awtar-Imam Muhammad Ibn Ali Ibn Abd Allah Al Shawkani Al Hanbali.
Nihayat Al Muhtaj Imam Shams Ad Din Muhammad Ibn Ahmad Al Ramli Al Shafii.
Nail Al Raja' Fi Sharh Safinat Al Naja Imam Al Bakar Al Dimyati AlShafii.

Rawdha An Nadhir Sharh Kaafi Al Mubtadi - Imam Abd Rahman Al Bali Al Hanbali.
Sharh Umdat Al Ahkami, Imam Muhammad Ibn Ahmad Ibn Al Imad Al Aqfahsi Al Shafii.
Sharh Sahih Muslim - Shaykh Ul Islami Imam Abu Zakarriyah Yahya Ibn Sharaf An Nawawi.
Sharh Al Kabir Al Shaykh Al Dardir wa Khashiyat Al Dasuqi - Imam Ahmad Ibn Muhammad Ad Dasuqi Al Maliki.
Sahih Al Bukhari - Abu ʿAbd Allah Muḥammad Ibn Ismaʿil Ibn Ibrahīm Al Juʿfī Al Bukhari.
Sahih Muslim - Imam Abū Al Ḥusayn Muslim Ibn Al Ḥajjāj Ibn Muslim Ibn Ward Al Qushayrī an-Naysābūr
Sahih Ibn Khuzaymah Abu Bakr Muhammad Ibn Ishaq Ibn Khuzaymah
Sunan Ibn Majah *Imam* Abū ʿAbd Allāh Muḥammad Ibn Yazīd Ibn Mājah Al Rabʿī Al Qazwīnī
Sunan Ibn Hibban*-Imam* Muḥammad Ibn Hibbān Al Bustī
Sunnan Abu Daud Imam Abū Dāwūd Sulaymān Ibn Al Ash'ath Ibn Isḥāq Al Azdī Al Sijistānī
Sunnan Al KubraImam Abū Bakr Aḥmad Ibn Ḥusayn Ibn ʿAlī Ibn Mūsā Al Khusrawjirdī Al Bayhaqī,
Sunnan An Nasai – Imam Abū ʿAbd Al Raḥmān Aḥmad Ibn Shuʿayb Ibn ʿAlī Ibn Sinān Ibn Baḥr Ibn Dīnar Al Khurasānī Al Nasāʾī

***Sunnan Al Daraqutni* –** Imam AlImam, AlHafidh, Al Mujawwid, Shaykh AlIslam, AlMuqri, Al Muhaddith 'Ali ibn' Umar ad-Daraqutni
Sunan Tirmidh– Imam Muhammad Ibn Isa At Tirmidhii Al Shafii.

***Talqah Al-Afham Al-Aliyah bi Sharh Al-Qawaid Al-Fiqhi* –** Shaykh Walid Ibn Rashid Al-Saidan.
Talkhis Al Kabir Fii Takhrij Al HadithAl Rafii Al Kabir - Mujaddid Ad din Shaykh Ul Islami Al Hafidh Imam Shihab Ad Din Abu Fadhil Ahmad Ibn Nur Ad Din Ibn Ali Ibn Muhammad Ibn Hajar Al Asqallani.
Tahqiq Qira'at Al Fatiha min Tabyin Aqwal Al Qadima Shaykh Muhammad Afifi Al Akiti.
Tabiyn Al Haqaiq Sharh Kanz Daqaiq - Imam Uthman Ibn Ali Al Zaylai Al Hanafi.
Tuhfah Al Minhaj Bi Sharh Al Minhaj - Al Muhaqqiq Imam Ibn Hajar Al Haythami.
Tarh Al Tathrib fi Sharh Al Taqrib - Al Hafidh Al Kabir Al Mutqin Al Muhariri Imam Zayn Ad Din Abd Rahman Al Iraqi Al Shafii.
Tuhfah Al Muhtaj - Imam Al Muhaqqiin Shaykh Ul Islami Imam Ibn Hajar Al Haytami Al Shafii.
Tuhfah Al Ahwadhi Bi Sharh Jamii Tirmidhii - Imam Muhammad Ibn Abd Rahman Ibn Abd Rahim Al Mubarakfuri Al Hanafi

Radd al Mukhtar - Imam Muhammad Amin Ibn Amr Ibn Abd Al Aziz Ibn Aabidin Al Shaami Al Hanafi.